
# BIBLIA

## YA

## WATOTO NA VIJANA



**Visa vya Biblia kwa Watoto na Vijana**

**Katika Mfumo wa Kesha ya siku 366 na Visa 407 vya Maandiko**

# BIBLIA
## YA
# WATOTO
## NA
# VIJANA

**Visa vya Biblia kwa Watoto na Vijana  Katika Mfumo wa Kesha ya siku 366 na VISA 407 vya Maandiko**

**BIBLIA YA WATOTO NA VIJANA**

**Ni masimulizi ya Biblia yaliyorahisishwa na kuandikwa kama Kesha ya siku 366.**

## MWONGOZO WA KUFUNDISHIA BIBLIA

**Fungu** la Kukariri
**Activity** kama Kuchora, kupaka rangi au mchezo wa kuigiza Nk
**Ombi** fupi

**Waandishi:**
Grace Momadi-Masaka
Daniel Nyangaresi Masaka
Daudi Jabez Masaka
Denis Momadi Masaka

**Email: masakamomadi@aol.com** **WhatsApp number: 1-908-343-3022**

## Yaliyomo

**1. Shukrani**

**2. Utangulizi**

**3. Jarida la Nyuma na Kuhusu Waandishi, na Wahariri**

**4. Machache Yahusuyo Biblia**

**5. Je, Tuliipataje Biblia ya Kiswahili?**

**6. Kwanini Tuisome Biblia?**

**7. Kesha ya siku 366**

**8. Rejelea**

**9. Farihisi**

**10. Vichwa vya Kesha zote 366-Yaliyomo kwenye kila kesha**

**11. Jinsi ya kuwa na adabu njema-Mambo 36**

**12. Vitafunio Safarini**

**13. Ahadi za Mungu**

**14. Mafundisho Makuu 28 ya Biblia-DOCTRINES**

**15. Malezi ya Mtoto wa Kike na wa Kiume**

**16. Masomo Muhimu ya Biblia kwa Wote (Bible studies) -Amazing Facts**

**17. Muhtasari wa Unabii wa Danieli na Siku zetu tunazoishi**

**18. Uwakili ni nini?**

**19. Masomo Muhimu ya Biblia kwa Watoto-Na Msafiri Mtenzi**

**20. https://www.adventistworld.org/365-days-with-jesus/ Soma Vitabu vyote vya injili kwa pamoja!**

**TABARUKU**
(book dedication)
1. Pastor Daniel Elfoard Matekere -Majita, Tanzania
2. Pendo Nyafanga Makori - Rorya, Tanzania
3. Denis Chilala Momadi - Masasi, Tanzania
4. Jemima Kivunge Nyafanga - Arusha, Tanzania
5. Paulina Bisieri Masaka - Kisii, Kenya.
6. Machwati Masaka- Kisii, Kenya
7. New Filipo- Malawi
8. Nyafanga Nicanor Makori-Mara Tanzania
9. Prisca Adongo Nyafanga-Migori, Kenya
10. Ana Jogoro na Chilala Momadi-Masasi, Tanzania

**Waandishi, Waombezi, Washauri, Teknolojia, Wahariri, Wasanii**
Grace Momadi-Masaka wa New Jersey, Marekani,
Daniel Nyangaresi Masaka wa Kisii, Kenya,
Bunga Dettu wa Lamadi, Tanzania
Stephen Letta wa Masasi, Tanzania
Kwandu Kasiri wa Kibaha, Tanzania
Gerard Odot Nyafanga wa Rorya, Tanzania
Faustin Momadi Mkama wa Dar-Es-Salaam, Tanzania
Mbusi Mpagalushu wa Bariadi, Tanzania
Daniel Matekere, wa Majita, Tanzania
Bettie Magesa Muasya wa Nairobi, Kenya
David Jabez Masaka wa Pennsylvania, Marekani
Paul Momadi Masaka wa New Jersey, Marekani
Obadiah Maina wa Nairobi, Kenya
Benard Chikowir wa Songea, Tanzania
Esrom Katuma, wa Mara, Tanzania
Annie Otieno Ouma wa Rorya, Tanzania
Innocent Wayoga, wa Dar Es Salaam, Tanzania
Dr and Mrs Wilson Trickett, wa Michigan, Marekani
Damas Kivunge, wa Arusha Tanzania
Charles Muraguri wa Nairobi, Kenya
**Ombea Huduma ya Vitabu Mtandaoni Uhamishoni Ughaibuni**
**Swahili Lulu for Immigrants and Refugees.**
**Toleo la Kwanza: Linaenda kwa Uhariri namba 3**

**Vitabu Vingine Kwenye Mlolongo huu wa Swahili Biblia Project RYU-Runinga ya Upendo**
1. Pdf ya Biblia ya kawaida na Biblia ya Kronolojiko ya Swahili Word Project/ Swahili Biblia ProjectRYU
2. Nipe Biblia- Muhtasari wa Vitabu 66 vya Biblia.
3. Afya Yako.
4. Mwanamke Anayempenda Bwana
5. Mlei Ni Nani (Hasa kwa Wanaume)- Kitabu Kizuri kwa Viongozi wa Kiroho.

6. Kulea Watoto.
7. Siri za Maombi.
8. Msingi wa Elimu.
9. Nyimbo za Pambano Kuu.
10. Shuhuda Kwa Kanisa, Magombo 10.
11. Ufafanuzi wa Biblia kutoka Blog, Agano la Kale na Agano Jipya.
12. MISINGI YA ELIMU KWA BINADAMU-Nyumbani, Shuleni na Taifani-must read kwa kila binadamu
13. Huduma kwa Wasiojiweza
14. Huduma ya Wachungaji
15. Mwulize Nabii
16. Mchoro uliovunjika-Broken Blue Print
17. Maisha ya Kustaafu
18. Mbinguni
19. Mashauri kwa Binadamu
20. Mashauri ya Chakula
21. Ukweli Kuhusu Malaika
22. Mashauri kuhusu Ngono, Uzinzi na Talaka
23. Mavazi Ya Kumpendeza Mungu.
24.Wafanyakazi wa Injili
25.Huduma ya Ustawi
26. Makambi
27.Huduma ya Uponyaji
28.Utume Kwenye Miji
29. Huduma ya Chakula
30. Shuhuda kwa Wachungaji na Watendakazi wa Injili
31. Kuombea Watoto Wako Kama Mwenda Wazimu
32. Habari za Kushangaza, Amazing Facts!
33. Historia ya Watu Wachache Waliotetea imani Tanzania

**Na vinginevyo**
Hii ni Edition ya kwanza, imehaririwa na inangoja kuhakikiwa. Ukiwa na mashauri, au masahihisho tafadhali usisite kutufikia ili tufanye utume pamoja, tuombeane sana ili Waandishi wenye uzoefu katika ulimwengu wetu wa Kiswahili wasaidie kutoa mashauri yenye uzima na hivyo kufanya mengi yapatikane bure au kwa bei unafuu. Tuombee katika huduma hii tunapofikiria kuandika vitabu vya watoto, kupata watu ambao wana uzoefu wa kufanya hili kwa lugha ya Kiswahili na kusaidia kuchapa. Tunatamani maombi yenu katika huduma hii ya Vitabu Mtandaoni Uhamishoni Ughaibuni

**MARANATHA**

**Shukurani:** Hatuwezi kusema kwamba hiki ni kitabu chetu, la hasha, maana mengi tumepata kwa watu wengine, zaidi ya sisi, yaani mimi, mume wangu, wahariri na watoto wetu. Nimebarikiwa na Wahariri wetu- Bunga Dettu, Daniel Matekere, Stephen Letta, Kwandu Kasiri, Mbusi Mpagalushu, Bettie Magesa-Muasya, Innocent Wayoga, Gerard Makori Nyafanga, Faustin Mkama, Obadiah Murimi na Charles Muraguri, Gerard Nyafanga, Faustin Mukama, Bariki Milinje Momadi, na Benard Chikowir amekiweka kwenye sauti na kiko Youtube Mtandaoni: **Kesha la Asubuhi (Watoto & Vijana) huduma ya Kijito cha Uvuvio.** Nimezungumza na walei, wachungaji, na waumini mbalimbali ambao wameonyesha kuvutiwa na wazo la kitabu hiki. Hivyo kitabu hiki kitakuwa ni baraka kwa watu wote. Ni naia yetu kukiweka mtandano bila malipo na kukichapa pesa zinapopatikana. Kiswahili sasa yaonekana ni lugha ya 3 kwenye ulimwengu wa Kikristo na 10 kwenye lugha zote duniani, ni maombi yetu tupate Ufafanuzi wa Biblia, na Kamusi za Biblia (Bible Commentaries, na Bible lexicons/concordance). Kiko mbioni kutafsiriwa na kuchapwa! Ombea Mambo haya ya **Injili Swahili Uhamishoni Ughaibuni!**

Je, tunawezaje kuelekeza nia zetu au kushinda majaribu? Kwanza, ni kwa kumchagua Mungu. Kama Yoshua alivyosema 'Chagueni hivi leo ni nani mtakayemtumikia!', kisha kwa kusoma na kuishi sawasawa na Maandiko ili tusitende dhambi - Zaburi 119:10; pili, ni kwa kumpinga na kumkimbia Shetani - Yakobo 4:7; na tatu, kwa kutafakari yote yaliyo mema, yaliyo bora, na yenye habari njema kama inavyosema katika kichujio cha pekee na bora cha Wafilipi 4:4-8, hichi ni kichujio cha yote na wote wenye mwili. Kisha 2 Wakoritho 5:10 inasema "tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo." Basi Neno la Mungu si Kitabu cha kupata habari au elimu tu bali ni Kitabu cha kubadilisha tabia zetu zifananane na tabia ya MUNGU, ili tuweza kujitoa kikamilifu (Bible is not a book of information but of transformation). Hebu Roho Wake Bwana, atusaidie tujiweke wakfu. Tukijitoa wakfu kikamilifu twaweza kufikia watu bilioni tatu ambao hawajui kuhusu ujumbe wa Masalio, wa Mungu hai wa mbinguni Ambaye alituumba, akatufilia na anakuja kutuchukua tuishi Naye milele. Maisha ni mafupi sana, Maandiko yasema miaka 1000 kwa Mungu ni kama siku moja tu, hii inamaanisha kwamba Adamu aliishi kama masaa 20 hivi tu, na mtu leo akiishi miaka 80 atakuwa ameishi masaa mawili tu hivi! Hii inatubidisha tuutafute ufalme wa Mungu na haki Yake, kwamba Maandiko haya yasitoke machoni petu bali tuyatafakari usiku na Mchana, maana yana Uzima wa Milele!
Tabia na wale tunaowapenda ndivyo vitu pekee yake tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, "Njoo!" Kila mtu asikiaye hili, na aseme, "Njoo!" Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina.
**Habari Njema Uhamishoni Ughaibuni**

Samaritan Laymen Ministries of Jersey.

***Mafundisho ya Biblia kwa Watoto***

Biblia Sahili- Kesha la siku 365 kwa watoto na watu wazima

**<u>Mambo Muhimu Saba tunapoendelea kusoma Biblia ni</u>**

1. Tumwamini Mungu, na kuungama dhambi zetu
2. Tusome Maandiko Kila Siku
3. Tusali kila siku
4. Tuhudhurie ushirika unaofuata Maandiko
5. Tujishugulishe na huduma za jamii
6. Tuwaambie wengine habari njema
7. Tuishi Mtindo wa maisha w Maandiko tunayasoma

**UTANGULIZI**

Tulipotembelea sehemu nyingi za Afrika Mashariki, hatukupata kuona Biblia ya watoto, au visa vya Biblia ambavyo vimeandikwa kwa lugha ambayo inaweza kueleweka kwa urahisi kwa watoto na yenye kina. Jambo hili lilituumiza sana, na tulianza kuwaomba baadhi ya watu watusaidie kuandika kitabu kinachoweza kukidhi hitaji hili.Watu hao walitoa udhuru kama sisi tulivyofanya, mpaka tukaona kwamba ni vyema tuandike. Tulimwomba Mungu atumwagie Roho Wake na kutusaidia kuandika. Tuliwaomba wengi waendelee kutuombea. Tunamshukuru Mungu kwa uwezo Wake na jinsi anavyotuwezesha na kutubariki. Hakuna kitabu kinachotoa faraja na kumpatia binadamu furaha kama inavyofanya Biblia! Tunaishi dunia ya dhiki, mashaka, fadhaa, hofu, na hata huzuni nyingi; na watu wana shauku ya kusikia habari njema, Mungu ametuandikia habari njema na za matumaini. Habari Njema ni Yesu kuzaliwa, kuishi duniani, kufa na kufufuka, ili tupate wokovu. MUNGU kwa njia mbali mbali ametia moyo tusifadhaike, tusiogope, maana anatupenda sasa kuliko tunavyojipenda wenyewe. Anawapenda pia wale unaowapenda kuliko wewe unavyowapenda. Marafiki, pesa, vileo, filamu, michezo, wanasesere/toys, na hata familia havitakupatia furaha sawa na ile utakayoipata toka kwa Mwenyezi Mungu.

Katika Zaburi 121:2, inasema "Nitayainua macho yangu niitazame milima, msaada wangu utatoka wapi?" Njia ya Mungu pekee Ndiyo itakayokusaidia na kukupatia amani moyoni, roho ya kuridhika, na ya kuwa na malengo ya maana maishani. Endapo una shida, huzuni, mashaka, ugonjwa au lolote linaloleta huzuni, Neno la Mungu Ndiyo habari njema pekee! Ni jibu kwa matatizo yako yote. Lisome hili ugundue Maneno Ambayo yatakupatia furaha na malengo mema ya milele. Mithali 22:6 inasema "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha hata atakapokuwa mzee." Kimbilio letu katika malezi au usalama wetu ni Neno la Mungu. Biblia ni sauti ya Mungu KAMA VILE MUNGU ANAZUNGUMZA NASI USO KWA USO. Mbingu na dunia zitapita bali Neno Lake halitapita kamwe. Neno la Mungu halikuja kwa mapenzi ya binadamu bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na Roho Mtakatifu 2 Petro 1:21-19-21. Maandiko ni pumzi ya Mungu na tumepewa kwa makusudi ya kuhekimishwa, ili tupate wokovu kwa imani, tufundishwe, tuonywe makosa yetu, tuongozwe, na kuadibishwa katika haki ili tuwe kamili katika kila tendo jema. 2Timotheo 3:15,16. Neno la Mungu ni muhimu kuzidi chakula tulacho.

Tunajuaje kwamba Biblia ni Neno la Mungu au la Kweli? Kila mtoto anapaswa kujua jinsi ya kujibu swali hili kuhusu tumaini tulilo nalo. Kuna sababu nyingi, lakini sababu moja kuu ni kuwa: Maisha ya mamilioni ya watu yamebadilishwa kutoka dhambini na kuwa baraka kutokana na nguvu ya Neno hili. Hakuna mtu aliyesoma somo la Hisabati na kusema, "Baada ya kusoma hesabu, moyo wangu umeamua kuchagua mema au kuacha dhambi". Lakini wapo wengi ambao walifikia uamuzi huo baada ya kusoma na kujifunza Neno la Mungu. Jaribu kuchukua muda wako kusoma Daniel 2 na Daniel 7 ambao ni unabii sambamba uliotimia. Huu unaonyesha kwamba BIBLIA ni kitabu cha uhakika, na utabiri Wake ni wa Kweli tupu.

Neno la Mungu ni dira na ramani yetu hapa duniani. Neno la Mungu limefika kwetu kwa njia ya uvuvio. Uvuvio uliwaongoza watumishi wa Mungu kama ilivyokuwa kwa manabii kama Musa, Danieli aliyekuwa waziri mkuu, Sulemani na Daudi waliokuwa wafalme, Amosi aliyekuwa mchungaji wa mifugo, Mathayo aliyekuwa mtoza ushuru, Luka aliyekuwa tabibu, na wengine wengi. Kuvuviwa siyo imla, kwamba waliambiwa waandike herufi kwa herufi, bali mawazo yalivuviwa na wakaandika kwa uongozi wa Roho Mtakatifu. Kwa mfano, wengine waliandika kimashairi, wengine kama unabii, na wengine kwa njia ya visa. Biblia imethibitika kuwa ni Neno la Mungu. Hakuna kitabu kinachoweza kujibu maswali ya binadamu kama hichi. Hakuna kitabu kinachotuliza shauku na upweke wa mioyo ya watu kama Biblia! Biblia inatoa mwangaza wa maarifa na hekima, maarifa na ufahamu wa kuangaza fikira zetu na kututakasa. Ni mafunuo toka kwa Mungu Aliye Hai. Yeye ni Nuru ya Uhai wetu! Mungu amelitunza Neno Lake katika historia kwa maelfu ya miaka. Biblia ina Maagizo, Shuhuda, Sheria, na Amri za Mungu, soma Zaburi 119.

Biblia ina vitabu 66. Vitabu 39 vya Agano la Kale na 27 vya Agano Jipya. Ilichukua zaidi ya miaka 1700 kuiandika Biblia; hata hivyo, waandishi wote, wanaokadiriwa kuwa 40 walikuwa na mtiririko mmoja, na wala hawakupingana, maana walivuviwa na Mungu mmoja. Biblia ina sura 1189. Sura ndefu kupita zote ni Zaburi 119, na kitabu kirefu kupita vyote ni Yeremia, kisha Mwanzo, kisha Zaburi, Kisha Ezekieli na kisha Kutoka. Vitabu vifupi kupita vyote katika Biblia ni 3Yohana, 2Yohana, Filemoni, Obadia na Yuda Sura fupi kupita zote ni Zaburi 117. Zaburi 118 ndiyo sura ya katikati. Wakati Biblia hazijaanza kuchapishwa bado, nakala zaidi ya 23,000 zilipatikana sehemu mbali mbali duniani zikiwa zinafanana kabisa, tofauti na vitabu vitabu vingine vya zamani kama Plato, Socrates, hivi vilikuwa vichache kama, mara zingine pungufu ya kopi 10. Hii inaonyesha si kitabu ambacho kimegushiwa. Vitabu vya Matendo na Luka vilichukuliwa na kuchunguzwa miji, matukio, na tarehe, na kukutwa na uaminifu usioweza kuelezeka kwa maneno! *(authentic)

Biblia inaweza kugawanywa kutoka Mwanzo kwa jinsi ifuatayo: Vitabu vya Musa vitano, vitabu vya historia 12, vitabu vya mashairi vinne, vitabu vya manabii vikubwa vitano na vidogo 13, vitabu vinne vya injili, kitabu cha matendo na historia ya matendo ya mitume kimoja, nyaraka za Paulo 14 na nyaraka za mitume wengine 7, na mwisho kitabu cha unabii cha Ufunuo.

Kwa mujibu wa Biblia dunia yetu ina miaka kama 6000 hivi tu. Gharika ilitokea mwaka 2348 KK na kuzaliwa kwa Yesu ilikuwa miaka ya 4 KK - 1 BK. Biblia inaeleza wazi wazi katika Ufunuo 12 kwamba kulikuwa na vita mbinguni na Shetani alitupwa hapa duniani na kuwadanganya wazazi wetu Adamu na Hawa. Hapo ndipo dhambi ilipoingia duniani. Dhambi ni uasi wa Sheria za Mungu. Dhambi ndiyo ilileta maumivu, huzuni, kifo na vilio. Tukiungama na kuwa na toba ya kweli, Mungu ni mwaminifu, anatusamehe na kutufanya tuanze maisha mapya, ukrasa mpya. Pambano kati ya uovu na wema, au Shetani na Mungu linaendelea na litaendelea mpaka siku ya mwisho ambapo Kristo atakuja kuwachukua watakatifu Wake. Vita hivi ndiyo virefu kupita vyote. Vita vimechukua takribani 6000 na Shetani hajajisalimisha bado mpaka hivi leo. Vita vifupi kupita vyote vilipiganwa

**Vitabu Kumi vya Biblia vilivyoorodheshwa kutokana na urefu wake, ambavyo ni asilimia 55% ya Agano la Kale vipo hapa kwenye chati n a Vitabu vifupi ni Obadia, 2Yohana, 3 Yohana na Yuda.**

| Kipi Kitabu Kirefu | Kitabu | # Mafungu | Graph-unit Hits | Morph-unit Hits | Bytes |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Yeremia | 1,364 | 22,285 | 30,203 | 241,209 |
| 2. | Mwanzo | 1,533 | 20,722 | 28,848 | 226,894 |
| 3. | Zaburi | 2,527 | 19,662 | 25,465 | 238,562 |
| 4. | Ezekieli | 1,273 | 19,053 | 26,572 | 214,416 |
| 5. | Isaya | 1,291 | 17,197 | 23,204 | 191,777 |
| 6. | Kutoka | 1,213 | 16,890 | 23,934 | 184,372 |
| 7. | Hesabu | 1,289 | 16,583 | 23,363 | 182,945 |
| 8. | Kumbukumbu La Torati | 959 | 14,488 | 20,329 | 159,872 |
| 9. | 2 Mambo ya Nyakati | 822 | 13,520 | 20,000 | 154,125 |
| 10. | 1 Samweli | 811 | 13,506 | 19,211 | 147,392 |

kule Zanzibar, kwa muda wa dakika 38, na Sultani wa Omani, akasalimu amri ndipo Uingereza ikakichukua hicho kisiwa. Hatimaye, Mungu atafuta machozi ya watu Wake. Hakutakuwa na kilio tena, wala huzuni, wala kifo. Wale walioshinda kwa neema ya Mungu, wakimtegemea, wakimtii na kumtumaini Yeye watapata zawadi ya uzima wa milele. Hiyo ni zawadi kuu kupita zote duniani. Mpendwa mtoto na kijana, mtumaini Bwana na kumchagua kila siku katika maisha yako. Mambo Saba muhimu kwa kila binadamu ni, kwanza, kumjua Mungu na kufuata njia Yake, pili, kuomba kila siku, tatu, kusoma Neno Lake kila siku, nne, kuabudu wengine kwenye ushirika unaofuata Maandiko na tano, kushuhudia matendo makuu ya Bwana kwa wengine, na Sita, kusaidia katika huduma za jamii na saba, kuishi mtindo wa maisha yale ambavyo Maandiko yanatuambia. Jaribu kujua tofauti kati ya dhambi, uovu, uasi wa sheria, makosa (Sin, Iniquity, and transgression). Dhambi za kujua na kutojua, dhambi za kutenda na kutotenda, zote hizi Mungu anatusamehe, akitutaka tuanze kuishi maisha mapya tena.

Wengi ambao wamelisoma Neno la Mungu wamesema, “sijapata kuona uzuri na utamu kama huu”. Biblia itazidi kung’aa na kuwa dhahabu ya thamani kila siku unapoendelea kuisoma. Utamu Wake utakuwa wa ajabu, na wala hutapenda uache kuisoma! Jambo hili nimelishuhudia, maana niliomba ombi hili mwaka 1988, nilipoona mwalimu wangu toka Uingereza akisema, Neno lina utamu wa ajabu,

akasema asipolisoma asubuhi, anaona amepungukiwa furaha! Nami nikasema, Bwana naomba nami unipe ladha ya Maandiko aliyo nayo huyu Mwalimu wangu! Bwana ametimiza ahadi hii kwangu na zingine nyingi maishani mwangu. Biblia ina ahadi zaidi ya 8000!

Wengi waliokuwa na uwezo mdogo darasani wamefanya vizuri kwa kulisoma Neno hili. Watu wamejua mambo ya siku za usoni kwa kulisoma. Angalia kitabu cha Danieli 2. Sisi hatuhitaji mnajimu au mchawi, au wabashiri wa aina yoyote kutwambia yale ya wakati ujao, kwani watakuweka kwenye woga bila sababu. Soma Biblia, na usiviruke vitabu vya unabii wa Daniel and Ufunuo. Mtegemee Mungu kwa akili zako zote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe, katika njia zako zote. Mkiri Mwenyezi Mungu, Naye atakupitisha vyema katika yote, nawe siku moja utakuwa mbinguni, ili uishi Naye milele, shangwe ya ajabu itakuwa siku hiyo. Siku ya Bwana utasimama kama Mshindi kwani Yeye atakutetea kwa vile umemchagua Yeye na njia Zake. Utakuwa umejiepusha na dhambi na huzuni nyingi hakika. Siku hii ya Bwana imetajwa zaidi ya mara 22 kwenye Biblia, na tunaambiwa kwamba kila binadamu ajitayarishe kwaajili ya siku hii.

Binadamu wote tumepotoka na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, na mshahara wa dhambi ni mauti. Bali Mungu ametoa njia kupitia Kafara ya Mwana Wake Kristo. “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda Ulimwengu, hata Akamtoa Mwanawe pekee ili kila amwaminiaye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Mwana wa Adamu hakuja ili ahukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika Yeye” Yohana 3:16-17. Mpendwa mtoto, kijana au mtu mzima, tuna matumaini ya kwenda kuishi mbinguni milele na milele na Baba yetu wa mbinguni. Hebu tupige moyo konde, tumwombe atusaidie katika safari hii na tupate marafiki wazuri wasio na misukumo ya uovu, ili tushinde mbio hizi. Kutomtii Mungu huyafanya maisha yetu na ya wengine yawe na huzuni. Ni vyema tumtii Yeye bila kushurutishwa maana itatubariki, na kuwabariki wenzetu na kumbariki Mungu pia. Hatuwezi kugusa mbingu bila kugusa watu! Tunapomtendea mwenzetu ubaya, tunakuwa tumemtendea Mungu pia, Yeye ni Baba yetu sote. Mahusiano haya hayatenganishwi. Na hivyo Mungu anapotoa katazo kwa kusema “usi” ni kwaajili ya furaha yetu wenyewe, sisi ambao ni viumbe Vyake. Mfano anaposema usizini, Yeye hana mke, ila anatoa katazo kwaajili ya furaha yetu wenyewe. Maagizo na Amri Zake zote Kumi, ni kwa faida yetu wenyewe. Kila Maagizo Yake, ni kwa faida yetu na wenzetu! Waweza kufanya utafiti kwa kila agizo Lake zaidi! Nasi tunaendelea pia, tuombeane

Miaka 170 iliyopita kule Ulaya walitokea watu wa nadharia potofu za mabadiliko ya mwanadamu toka minyoo, chura, nyani na kisha binadamu. Nasi twajua hakuna aliyesikia redioni “leo tunakaribisha raia wapya toka msituni Gombwe au Virunga, ambao wamebadilika kutoka sokwe au nyani na kujiunga nasi!”. Hizi ni nadharia potovu, ovu na za uongo. Nafikiri sisi hatusumbuliwi sana na nadharia hizi kwa vile nyingi zinatupunguzia thamani ya utu wetu kama binadamu na kisha tunaishi na viumbe hivi kwenye mbuga zetu na hatuoni mabadiliko hayo. Hata hivyo tunaamini kwamba tumeumbwa na Mungu kwa Makusudi makuu. Biblia inasema tumeumbwa na Yeye Mwenyewe Mwenyezi Mungu, hebu tuachane

na ubunifu usio na utashi au Mungu ndani yake.

Tuisomeje Biblia basi? Wasomaji Wengi wapya wanasema hawajui waanzeje. Kuna njia nyingi za kusoma Biblia. Wengine wameanza Mwanzo wakaishia kwenye vitabu walivyoviona haviwapi shauku au matamanio ya kuendelea kusoma. Tunashauri kuanza vitabu vya injili kama Marko, Mathayo, Luka na Yohana. Kisha Matendo na kurudi kitabu cha Mwanzo na Kutoka. Unaweza kuisoma kwa kuchukua mtu mmoja na kujifunza maisha yake. Mfano, Stefano shemashi aliyempenda Mungu na maisha yake. Alikuwa mgiriki, hakuwa na roho ya kulipiza kisasi, aliwaombea waliokuwa wakimwua. Watu wengine wakifanyiwa kosa dogo hutoa mwitikio wenye jazba, na kusema "hata nikifa, usije kwenye mazishi yangu, utalaaniwa kwa kunitendea ubaya huu, utakuwa masikini wa kutupwa" Maneno haya ni mazito sana. Wale wanaotutendea mabaya, tunapaswa kumwomba Mungu awasamehe na kutuepusha na shari yao. Waweza pia kuinakili au kuifanyia muhstasari kama sasa tunavyofanya, jambo ambalo limetufungua macho kwa njia tusiyoweza kuelezea. Utakapozoea utaweza kuanza mwanzo mpaka mwisho kwa urahisi kama ambavyo wengine wetu tunafanya. Soma sura tatu kila siku na kwa mwaka utakuwa umeimaliza. Au kila siku soma sura moja na kutafakari na utamaliza baada ya miaka mitatu. Zungumza na wengine kuhusu namna wanavyoisoma. Jitahidi uisome kwa furaha na kuomba uvuviwe na Roho wa Mungu, kabla hujaanza. Na kila unapoanza kuisoma, omba na omba tena! Utabarikiwa na faida kemkem. Usijipangie kusoma kurasa nyingi ambazo zitafanya uone kuwa ni adhabu au utakazoshindwa kuzimeng'enya vyema. Biblia ni kama chakula. Chakula kinatakiwa kutafunwa na kuyeyushwa, ndipo unapata lishe. Kusoma Bibla yote inachukua saa kama 80 tu. Lakini unahitaji muda wa kuomba na kutafakari hata fungu moja tu, utashangaa kwamba linaweza kukuchua wiki mbili! Usifanye kwa kasi kana kwamba unashinikizwa au unakimbizwa. Biblia ina Ujumbe kwa watu wa tabaka zote, wazee, vijana, matajiri, masikini, weusi, weupe, wafupi, warefu, wasomi, na watu wa kawaida.

Kamwe Tusihofu, Neno linasema, "Usiogope, kwa maana Mimi ni pamoja nawe, usifadhaike, kwa maana Mimi ni Mungu wako, Naam, Nitakutia nguvu, naam Nitakusaidia, Nitakushika, naam, Nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki Yangu" Isaya 41:10. Kweli macho hayajaona, wala masikio kusikia wala kuingia katika mawazo ya mwanadamu, Mambo yale ambayo Mungu ametutayarishia!" Hebu tusome Neno Lake ili tuzijue ahadi maelfu na kuzidai.

**Jarida la nyuma**

Dini ya Kikristo hairuhusu mtu kufanya atakavyo! Muumini anapaswa kujisalimisha kwa Mungu na kuishi sawasawa na Maandiko. Kabla ya dhambi Mungu alizungumza na watu uso kwa uso, lakini baada ya anguko dhambini alitumia Maandiko. Biblia ni Neno la Mungu. Neno la Mungu ni mamlaka ya mwisho kwa viumbe wa Mungu hapa duniani, Na mbinguni na lina Ujumbe kwa kila mtu. Lisome, litafakari, lipende, litende, litangaze, liangaze. Usizuie wengine kulisambaza au kuwa choyo nalo. Maana utume wetu ni kuenenda katika ulimwengu wote na kuwafundisha watu, na kuwafanya kuwa wafuasi wa YESU

Kitabu hiki ni masimulizi ya Biblia kwa watoto kuanzia kitabu cha Mwanzo mpaka Ufunuo katika mfumo wa somo la kila siku kwa siku 366.

Biblia inatueleza Historia ya Binadamu toka alipoumbwa na Mungu, mpaka kuanguka na kuasi sheria za Mungu pale katika Bustani ya Edeni mpaka Mungu atakapofanya makao Yake pamoja Naye katika mbingu mpya na nchi mpya (Uumbaji, Maanguko, Ukombozi). Kuna Neno linaitwa kigiriki Theodicy (theodisi) Katika kitabu cha Ufunuo 12 tunaelezwa kwamba, Shetani aliishi mbinguni na kuwa mwasi wa kwanza. Alishawishi theluthi ya malaika wote na kutupwa nao hapa duniani. Huo ukawa ndio mwanzo wa pambano kati ya Mungu na Shetani, au wema na ubaya. Kwa sasa tumo katika pambano hili, kitabu cha Ayubu kinatupatia picha kidogo ya pambano hili. Kuna siku pambano hili litakwisha. Kutokana na Biblia, ishara za nyakati katika kitabu cha Danieli sura ya pili na saba ni kalenda ya unabii. Hii inaonesha tuko ukingoni mwa Historia ya Dunia hii. Mungu atakuja kuhukumu ulimwengu, na kutoa thawabu kwa wale waliotenda mema kwa neema Yake, yaani, uzima wa milele; na kwa wale waliotenda maovu, adhabu yao ni moto wa milele. Kila mtu na asome sura hizo za Daniel na kujua maana yake ni nini Leo. Huu ndiyo muhtasari wa Biblia. Mwanzo 1 na 2 ni uumbaji, Mwanzo 3 ni kuanguka kwa binadamu dhambini. Biblia yote iliyosalia baada ya hapo ni mpango wa Mungu katika kuishughulikia dhambi ili isiinue pembe yake kamwe tena. Nahumu 1:9. Anatuma mitume na manabii kusaidia watu kujitayarisha, mara nyingi watu hawasikii, na mara zingine wanaua wale watumishi wa Mungu, hatimaye Mungu anamtuma Mwanawe Naye anazaliwa, na kuishi na watu miaka 33 1/2 na kuwafundisha watu, mwishowe anauwawa, na kuzikwa na kufufuka na kupaa kurudi mbinguni, akiwa na huduma ya ukuhani kutuombea, na hivi karibuni atatokea kuwachukua wale waliofanya uamuzi kuishi Naye mbinguni milele, na adhabu itatolewa kwa wale ambao wamekuwa hawampendi Yeye, na hawapendi watu wengine.

Mimi na wewe mtoto ama mtu mzima tumo kwenye pambano hili zito. Hata mtoto mdogo anapata shida kujikana nafsi, au kujinyima, na kutaka yote yaende anavyopenda. Mapambano yote yapo kichwani na moyoni, tunasikia sauti mbili moyoni. Imetupasa tuvae silaha za Mungu na kusimama imara, soma Efeso 6 silaha zile Saba, tukeshe na kuomba ili tusiingie katika mitego na nyavu za yule mwovu. Kila siku tunafanya uchaguzi, ama tunamchagua Mungu au Shetani. Wote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, lakini tunapomwamini

Yesu na kutubu, Mungu anatusamehe na kutukubali kama watoto Wake. Mungu Anatusaidia kuishi maisha mapya kwa neema Yake.

Hebu tumwamini Mungu ili tuthibitike, na tuamini manabii Wake ili tufanikiwe. Kitabu hiki kimebadilisha maisha ya watu wengi. Wakoloni walipofika kule Papua New Guinea waliwacheka wananchi waliokuwa wanasoma Biblia na kuifuata. Wale wananchi wa Papua New Guinea wakawaambia, "Mnacheka na wakati tulipokuwa hatuna kitabu hiki tulikuwa tunakula watu? Ninyi leo mngekuwa kitoweo chetu!".

Bwana Yesu Alisema, "Imeandikwa mtu hataishi kwa mkate tu! Bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu". Mathayo 4:4. Kwa neema ya Mungu, hebu siku moja tukutane mbinguni kando ya mti wa uzima kwa kuwa tumelithamini Neno Lake.

## Uandishi

**Grace Momadi-Masaka** Alizaliwa Bariadi, mkoani Simiyu, Tanzania. Ni mwalimu wa biolojia, kemia na uuguzi. Ana shauku ya kuandika vitabu vya watoto ili wamjue Mungu anayewapenda sana, na mwenye mipango ya kuwapatia maisha bora na kisha uzima wa milele mbinguni. Anaishi New Jersey, Marekani, na ana watoto wawili Daudi na Paulo. Anahimiza ibada ya nyumbani pamoja na watoto iwe ya kila siku asubuhi na jioni, na kusoma Neno la Mungu. Na kumsihi Mungu huruma na rehema Zake ili tutembee njia sahihi, na kuombeana kwa machozi mengi. Biblia hii ya watoto na vijana itasaidia wazazi kusoma pamoja na watoto wao. Anahimiza wale ***wanaowiwa kutafsiri*** mashauri ya tumaini ili kuufikia ulimwengu wa Kiswahili tutafutane kwa pamoja ili kutafsiri lulu nyingi kwa ulimwengu huu wenye maandishi machache. Email masakamomadi@aol.com

**Daniel Nyangaresi Masaka** alizaliwa Kisii, Kenya. Yeye ni mkemia wa viwandani. Anawasihi akina baba kujihusisha kwa karibu na watoto wao, na kujua kinachoendelea ili kuwasaidia watoto kwa maisha haya ya duniani na ya milele. Kazi ya baba kama kuhani na kiongozi ina thamani kuliko vile ambavyo inaelezwa katika maisha yetu ya kila siku. Hili ni muhimu hasa katika ulimwengu wa leo wa *kidigitali*, haswa baada ya Korona. Wengi tumefanya makosa, na kuomba rehema za Mungu kwani Yeye Ndiye Mzazi Mkamilifu. Wazungu husema kulea ni mwenye dhambi mmoja kumkuza mwingine (Parenting is one sinner raising another sinner).

**Bunga Edward Dettu** ni rafiki yetu wa siku nyingi, nimefahamiana naye kanisani nikiwa mwanafunzi kidato cha tano, hadi leo ni rafiki yetu tukisaidiana na kushirikiana kwa mambo mengi. Ametoa mchango mkubwa katika kitabu hiki cha Mafundisho ya Biblia, Yeye pia ni mwanazuoni, aliye na Shadaza za Mahusiano Kati ya Wakristo na Waislamu kutoka Chuo Kikuu cha Andrews. Mke wake anaitwa Theopista, nao ni wazazi waliobarikiwa kupata watoto watatu na wajukuu watatu. Kazi yake ni uchungaji.

Daudi na Paulo Masaka ni watoto wanaoishi na wazazi. Wao ni wanafunzi wa shule ya Msingi na wanasema, “Neno la Mungu sio tu mashauri au mawazo bora, bali ni sauti au pumzi ya Mungu na mamlaka ya mwisho kwa watu Wake duniani”. Wanashauri watoto wote walipende Neno la Mungu, walisome, na kulitenda; wakiomba nguvu toka kwa Bwana maana hakuna awezaye kufanya Mapenzi ya Mungu au kushika Sheria kwa uwezo Wake m wenyewe.

**Mbusi Mpagalushu:** Amesomea utabibu, na atoka Bariadi, Tanzania, asema, sisi Hatutaokolewa kwa Sheria bali kwa kafara kuu Ambayo Mungu aliitoa kupitia kwa Mwanae Yesu Kristo, lakini tutahukumiwa kwa Sheria! Wayahudi wengi walishika Sheria pasipo kumpenda Mungu. Lakini siku hizi, wapo watu ambao wanadai kuwa wanampenda Mungu ila hawazijali Sheria Zake. Hebu tuepuke unafiki, maana hilo ni jaribu letu sote binadamu. Yaani kuwa wanafiki au kuwa watu wa dunia, kwa neema tuwe watu wa Mungu.

**Kwandu Kasiri:** Kwandu amesomea mambo ya famasia, na anaishi kibaha, Tanzania, naye asema Je, unakiamini kitabu Biblia, ambacho ni Kitabu kikuu kuliko vyote (Kitabu cha vitabu). Je, unakisoma, na kuacha ujumbe Wake uzungumze na moyo wako? Ukifanya hivyo, utakuwa mtu tofauti. Kama ulikuwa hujakiamini, anza kukiamini leo, na kama unakiamini bila kukitii, anza kukitii leo, na kama unakiamini na kukitii, endelea kukua ukizaa matunda yanayopasa toba.

**Mchungaji Daniel Matekere:** alikuwa Mwalimu wa Biblia. tabibu na mhariri wa vitabu pia

Mchungaji Stephen Letta: Yeye ni mwalimu wa Biblia, mwandishi, na mhariri wa vitabu pia

## NIPE BIBLIA ---JE BIBLIA ya KISWAHILI ILITUFIKIAJE?

**Pricilla Owens**
**Nyimbo Za Kikristo No. 52: Nipe Biblia**

1.Nipe Biblia nyota ya furaha, wapate nuru wasafirio;
Hakuna la kuzuia amani,Kwani Yesu alituokua.

Nipe Biblia Neno takatifu,
Nuru Yake itaniongoza;
Sheria na ahadi na upendo,
Hata mwisho vitaendelea.

2. Nipe Biblia nihuzunikapo ikinijaza moyoni dhambi;
Nipe Neno zuri la Bwana Yesu, Nimwone Yesu Mwokozi wangu.

3. Nipe Biblia nipate kuona, hatari zilizo duniani;
Nuru ya Neno Lake Bwana Yesu, itaangaza njia ya Kweli.

4. Nipe Biblia taa ya maisha; Mfariji tunapofiliwa;
Unionyeshe taa ya mbinguni, Nione utukufu wa Bwana.

Kuna Wimbo umesema hata kama bahari zote zingekuwa wino, mbingu zote ziwe karatasi na miti yote iwe kalamu, zisingetosha kuandika habari njema za ufalme wa Mungu na upendo Wake. Tunasema hatujaanza hata safari ya kuuelewa upendo wa Mungu, kuelewa Neno Lake na kwamba Yeye ni nani, tumepata mnuso kidogo tu, lakini hata hilo dogo tulilolipata, tukilitia maanani litakuwa la matunda mema, tele na kisha Ahadi za ajabu za uzima wa milele kwa kumjua Yeye0-Yohana 17:3,
Biblia ni Kitabu cha kusomwa kwa kicho na heshim, kwa maombi na bila haraka, hebu Mungu atusaidie kukifurahia chakula bora na chenye ladha kupita vyote duniani ili tukue kiimani na kumtukuza Mungu, na kuboresha wengine kwa huduma na maneno yetu.

Kwasababu ya mafundisho mengi yasiyo ya Kweli, na yanayomdhalilisha mwanadamu, yanayotokezea kizazi hadi kizazi, hakuna aliye salama bila Neno la Mungu. Viumbe vyote wakiwemo malaika wameumbwa na Mungu. Mungu alimwumba Mwanamume kwanza, na kumpa kazi kwenye Bustani ya Edeni (pleasure/luxury). Adamu alikuwa na mahusiano na Mungu kwanza, kabla ya mahusiano mengine. Kisha akamwumba mwanamke aliyekuwa na mahusiano na Mungu kwanza na kisha mumewe alipokabidhiwa kwake. Amri ya zaeni na kuongezeka ni amri ya kwanza inayosomeka kwenye Maandiko! Mtoto anaumbika tumboni kwa mbegu toka kwa baba na yai toka kwa mama. Mbegu hizi mbili zinapokutana, mtoto hapo ndiyo mtoto anakuwa msichana au mvulana. Kwa hizo seli mbili. Nazo hukua. Hivyo mtoto hazaliwi msichana au mvulana tu, bali huumbwa na Mungu kama msichana au mvulana! Hakuna anayeweza kujibadilisha jinsia, maana kila seli ina vinasaba vya kike au vya kiume. Binadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Hivyo jinsia zote zina maana yake kwa Mungu. Hivi majuzi

nadharia toka nchi nyingi zimekuja na mambo mengi ambayo yameacha taabu nyingi. Pale napoishi kuna watu mtoto akizaliwa hauruhusiwi kusema ni msichana au mvulana, bali wanakwambia, wacha akikua mwenyewe atachagua. Mara nyingi pia nikienda kutumia choo wakati wa kusafiri kwenda majimbo mengine, shuleni au uwanja wa ndege, nakutana na wanaume chooni, ambao wanasema wao wanajisikia vichwani mwao ni wanawake. Hali kama hii hunipa hofu kama nipo peke yangu na mwanamume huyu chooni, Je, kama wewe ni mwanamke usingekuwa na hofu kweli? Habari za namna hii ni nyingi napoishi, ila kwa kifupi niseme, Mungu ameumba wanaume na wanawake kwa utufu Wake. Yeye Ndiye anaamua nani awe mwanamume na nani awe mwanamke, na si wanadamu. Mwanadamu hawezi kuumba. Kitenzi cha kuumba ni mojawapo ya vitenzi vinavyomhusu Mungu tu. Kitenzi kingine ni kusamehe dhambi n.k.

Sisi kama viumbe hatuna uchaguzi wa kuchagua tuwe watoto wa kike au wa kiume, tuwe weupe au weusi nk. Mungu alishaweka hayo yote kwenye vinasaba vyetu, kwenye kila seli (DNA). Nasi tumeumbwa kwa jinsi ya kushangaza na kutisha. Yapaswa tujue basi Mungu ametuumba kwa makusudi gani, kwasababu kila mtu atatupa *mashauri yake*, yaliyopotoka au yasiyopotoka, bali sisi na watoto wetu twapaswa kurudi kwa Mungu Mwenyewe kwanza, aliye na maelekezo ya kile alichokiumba (Manual). Biblia ndiyo Mwongozo huo wa maelekezo kwa Wanaume na Wanawake. Wao wameumbwa kwa malengo tofauti, wako sawa mbele za Mungu, ila kazi yao ni tofauti! (equal with different function)

## BIBLIA YA KISWAHILI ILITUFIKIAJE? (HOW DID WE GET SWAHILI BIBLE?)

Mary Jones alizaliwa kijiji cha Llanfihangely Pennant, katika kisiwa cha Wales (UK) tarehe 16 Desemba,1784. Alilipenda sana Neno la Mungu na alitamani sana awe na Biblia yake mwenyewe lakini alikuwa masikini. Akiwa na umri wa miaka 16, tayari alikuwa ametunza pesa ili aweze kununua Biblia yake mwenyewe, Alipata taarifa kuwa katika kanisa fulani, angeweza kununua Biblia, kwa hivyo, alitembea Km 40 kwenda kwenye kanisa ambapo alikutana na mchungaji Thomas Charles. Mchungaji alimweleza kuwa Biblia zote zilikwisha nunuliwa na haikusalia hata moja.


Mary alimsimulia mchungaji Thomas kisa chake na jambo hili lilimsisimua mchungaji kiasi cha kuamua kumuuzia Biblia ambayo ilikwisha lipiwa na mtu mwingine ila alichelewa kuichukua Biblia yake. Mchungaji huyu, alipata msukumo moyoni kufanya mpango ili watu wote wa kawaida wapate Biblia zao wajisomee kwa kuzingatia ule usemi usemao, “Uzima wa Milele ndiyo huu, Kumjua Mungu Mmoja wa Pekee na Yesu Kristo Aliyemtuma”.

Mchungaji Thomas alifanya mkutano na viongozi wa Religious Tract Society mwaka 1802, na katika mazungumzo waliafikiana kuisaidia Wales kupata Biblia. Baada ya maamuzi hayo, akatokea bwana mmoja aitwaye Joseph Hughes na kuhoji: “Yaani kwa Wales tu? Je, nchi zingine?”. Hoja zake zilipelekea kuundwa kwa

chama kilichojulikana kama, British and Foreign Bible Society, mnamo March 7, 1804. Kwa pamoja walianzisha mitambo ya kuchapa; ni kutokana na chama hiki vimezaliwa vyama vingi duniani vya Biblia vikiwemo kile cha Kenya Bible society, Bible Society of Tanzania na American Bible Society. Vyama hivi vimesaidia sana kueneza Biblia kwa wingi wakiruzuku mauzo Yake na  wakati mwingine hupata wafadhili.

Mary Jones aliishi miaka 80 na  alifanikiwa kushuhudia na kufurahia matunda ya njozi yake Mara nyingi tunadhani kuwa, mtu anaweza tu kuleta tofauti katika jamii iwapo ana pesa au mamlaka. Hapa tumeona kwamba hili si kweli, njozi inaleta malengo, madhumuni na hatimaye, yaweza kuhamisha milima mingi katika maisha ya mwanadamu.

Johannes Ludwig Krapf alizaliwa nchini Ujerumani (1810-1881). Alihitimu shahada ya Theolojia katika chuo kikuu cha Tubingen mnamo mwaka 1874. Alisafiri kwenda nchini Misri na huko alioa na kupata mtoto; Baadae, yeye na familia yake, walihamia  kule Rabai, Mombasa ambapo mkewe na mtoto walifariki kwa malaria. Krapf alikuwa na talanta ya lugha iliyomwezesha kufahamu Kigiriki, Kilatini, Kiebrania, kifaransa, na Kiitaliano. Krapf alikuwa Mlutheri na Mwaka 1844 alifanya umishonari  katika nchi za Afrika Mashariki. Mara alipowasili, mwaka 1844, alianza kujifunza Kiswahili cha kimvita. Aliandika Kamusi ya Kwanza ya Kiswahili na Sarufi ya Lugha ya Kiswahili.  Alianza pia kuandika kitabu cha Mwanzo cha Biblia ila lugha Yake haikuwa ns mpangilio mzuri (*Tazama mfano hapo chini hapa)*. Krapf aliona kwamba kuna mahitaji makubwa ya kueneza Neno la Mungu kwa watu kwa kusoma Biblia ya Kiswahili. Hata hivyo, jaribio hilo lilishindwa kwa sababu yeye mwenyewe alijifunza tu Kiswahili cha mawasiliano rahisi, ila hakuwa mtumiaji mzuri (tazama aya zifuatazo hapo chini))
Johann Krapf's 1847 tafsiri ya Mwanzo 1:1-3 into Swahili


In the beginning created God the heaven and
1. Mooanzo alioomba Mooigniazimoongo oowingo na
the earth.
n'tee.

And was earth without form void darkness
2. Yalikooa n'tee aina oozooree na toopoo ; yalikooa keeza
upon depth and the spirit of God was
katika shimo na roorkhoo ya Mooigniazimoongo yali
moving water.
ikipepēa katika madjee.

Said let there be light and there was
3. Alinēna Mooigniazimoongo, iwa nooroo, ikāwa
light.
nooroo.

Published in the Journal of the American Oriental Society, Vol. 1, No. 3, 1847

Krapf alifanya kazi na Jaji wa Kiislamu aitwaye Ali Bin Modehin, kutafsiri kitabu cha Mwanzo. Mwishowe, alimaliza Agano Jipya la kimvita japo hakuchapa nakala nyingi. Kazi yake ilikuja kutumiwa baadae katika kuandika Biblia ya Kiswahili " Southern Version" aliyoshughulikia Steer. Huyu katika mwaka wa 1868 alimaliza Agano Jipya na Mwaka 1879 Biblia yote ilikamilika, yaani, Agano la Kale na Agano Jipya. Waandishi wengine walikuja na kujiunga naye wakasaidiana kukamilisha uandishi wa Agano la Kale nao ni Johannes Rebmann, na Rabai Krapf. Majina ya wengine ni Wiliam Taylor, Harry Bins, Edward Steere, Franciss Hodgson, na Arthur Madan. Hadi kufikia mwaka 1895 Biblia yote ya Kiswahili iliweza kupatikana. Kamusi ya Krapf pia ilisaidia wengi katika kazi za kutafsiri. Krapf alitafsiri Biblia pia kikamba, na lugha ya Oromo ya Ethiopia.

Edward Steer (1928), Mwanglikani kutoka nchini Uingereza, aliwekewa mikono ya Uchungaji mwaka 1850. Alifika kufanya kazi Zanzibar mwaka 1864. na mwaka 1869 akiwa na Chapa ya Krapf alimaliza kutafsiri Agano jipya. Akisaidiana na Mwananchi Mzanzibari. Hawa walifadhiliwa na chama cha Biblia nao wakafanikiwa kutafsiri Biblia kwa lugha ya Kiswahili. Steer alikufa mwaka 1882.

Tafsiri aliyoianzisha Krapf iliendelea kuboreshwa na watu mbalimbali kwa kadri Mungu Alivyowatumia hadi mwaka 1950. Kamusi yake ilisaidia katika kutafsiri Biblia kwa Mchungaji Steer na wenzake na pia kwa tafsiri za makabila mengine ya kibantu kama Luganda. Chapa ya kwanza ya Biblia ya Kiswahili (tunayoitumia leo) ilitolewa rasmi mwaka 1952, hata hivyo kulingana na taratibu za mabadiliko na kukua kwa lugha, ni jambo la kawaida kuhakiki kitabu kila baada ya miaka 50. Wapo watu wengine wa Zanzibar ambao walisaidia kupata lugha sahihi hasa watunga mashairi kama vile Mwajuma, Shaban Robert na Mathias Mnyampala. Mchango wao ni tunu kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, Biblia yetu hii, ina umri wa miaka takribani 74, hatutashangaa iwapo siku moja tutapata Biblia fafanuzi au Biblia ya Kesha (Paraphrase/Devotional Bible). Tumeanza kuandika kitabu cha Warumi kwa ufafanuzi/Kesha (paraphrase/devotional) Hebu Mungu Atusaidie na kututumia ili kazi ikamilike mapema. Tunatamani maombi yenu. Tunaomba mtukumbuke katika utume.

Marekebisho ya mwaka 1950 yalizingatia umuhimu wa kuwa na "Standardized Bible" ya Kiswahili katika Afrika Mashariki ndipo ikazaliwa tafsiri ambayo tunayo mpaka leo (Swahili Union Version).

Makanisa mengine yameshiriki kutoa tafsiri ya Biblia ya lugha zingine za Afrika mashariki za makabila ya Afrika Mashariki, baadhi yake ni Mazumo (Zaburi) kwa lugha ya Chasu (Kipare) kilichochapiswa na Max Poenig Msabato mwaka 1919, Agano Jipya kwa Kipare mwaka 1912 na miaka iliyofuatia. Vingine vilivyofuata ni Agano la Kale na Agano Jipya (Ilagano lya Kale na Ilagano Ipya) kwa Kisukuma kilichotafsiriwa na Wamisionari Wasabato wa Kipare huko Usukuma wakati wa vita ya kwanza na kuchapishwa huko Kendu Bay (Kenya). Pia Mmisionari Rudolph Reider aliyekuwa Majita na Ibrahimu Maradufu walitafsiri Agano Jipya kwa lugha ya Kijita liitwalo Indagano Inyaaya baada ya vita ya kwanza.

Hapa kwetu barani Afrika, Chama cha Biblia kilifika nchini Kenya na Ethiopia kwanza, na wakati huo Tanzania tulihudumiwa kutokea Kenya mpaka mwaka 1978 chama hicho kilipoanzishwa hapa Tanzania huko Iringa. Kati ya 1979-1980 ndipo kilihamishiwa mjini Dodoma ambapo kimestawi hadi leo na kinaendelea kuhudumia jamii kubwa yenye mahitaji ya Neno la Mungu (hasa ilipoonekana kwamba kuna uhitaji mkubwa).
Kuna haja ya kuwa na tafasiri zingine za Biblia kama lugha zingine zilivyo, mfano Kingereza kina tafsiri zaidi ya 100. Sasa hivi kuna tafsiri ya Biblia ya Kiswahili cha Kisasa ambayo tumeshaizoea!
(Tumehoji vyama vya Biblia pia, ila kazi ya binadamu mara nyingi inakuwa na makosa, ila nia yetu ni kushiriki nanyi habari hizi njema hivyo kama kuna masahihisho yoyote tafadhali tusaidieni. Tunapenda kubarikiwa nanyi kwa maombi, mashauri na masahihisho, Asante).

Ombi zito sana ambalo limesheheni ni hili, nawe jiombee na liishi kisha utapata mafunuo ya kuweza kulielewa Neno na siku moja tuwe mbinguni pamoja NAYE milele zote,
Raha hiyo ya rohoni ni amana ya pumziko ambalo limewekwa juu kikomo cha masukumbuko!

**Efeso 3:14-20-Kwa sababu hiyo, nampigia magoti Baba, 15aliye asili ya jamaa zote duniani na mbinguni. 16Namwomba Mungu, kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, awajalieni kwa uwezo wa Roho Wake, nguvu ya kuwa imara ndani yenu, 17Naye Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani. Namwomba mpate kuwa na mzizi na msingi katika mapendo 18kusudi muweze kufahamu pamoja na watu wote wa Mungu jinsi upendo wa Kristo ueneavyo kwa mapana na marefu, kwa kimo na kina. 19Naam, mpate kujua upendo wa Kristo upitao elimu yote, mjazwe kabisa utimilifu wote wa Mungu.**

**20Kwake Yeye ambaye kwa nguvu Yake ifanyayo kazi ndani yetu aweza kufanya mambo makuu zaidi ya yale tuwezayo kuomba au kufikiria; 21Kwake Mungu uwe utukufu katika kanisa na katika Kristo Yesu, nyakati zote, milele na milele! Amina.**

**EFES0 3:14-21**

Grace Momadi-Masaka, David Bunga Dettu, Bariki Kangalu Elineema, na Daniel Nyangaresi Masaka 2012.

**Machache yahusuyo BIBLIA**

Biblia ni kitabu cha Habari Njema za wokovu wa kila mwanadamu. Muhtasari Wake ni uumbaji wa mwanadamu (Mwanzo 1 na 2). Maanguko ya mwanadamu dhambini (Mwanzo (3) na Biblia yote iliyobakia kuanzia Mwanzo tatu mpaka Ufunuo, ni Mungu anafanya juu chini kumwokoa mwanadamu, anamtuma Kristo kuja kutukomboa. Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, Kristo anakufa kwaajili yetu ili tuweze kuishi milele. Tunabadilishana Naye, Yeye anatupa Wema Wake, nasi tunampa dhambi zetu ili atusafishe kabisa, na kutufanya tustahili kwa haki Yake. Kitabu hiki ni cha ajabu, kwani mtu akisimulia maisha yake au ya marafiki zake huwa anasema mambo mazuri tu ya watu hao. Hata mtu mwingine ameshauri watu waishi vyema "ili usije ukatulazimisha kusema uongo wakati wa mazishi yako!" Ila Biblia haiko hivyo, habari za watu zimesemwa kama zilivyo, hata wale wapenzi wa Mungu! Hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja, wote tumepungukiwa na utukufu wa Mungu.

Biblia yazungumza ulimwengu ulivyokuwa, ulivyo na utakavyokuwa. Hakuna kitabu kingine chenye Ukweli wa haya kama hiki. Kitabu hiki ni tofauti na vitabu vingine vyote kwani hakuna kitabu kinachosema "Ndipo Mungu Akasema…. Au Sikiliza Neno la Mungu au ….. Neno la Mungu likanijia" Mtu mwenye hekima kamwe hatasema kuwa Mungu hayupo, bali atapeleleza naye atakutana naye, ***ni Ahadi ambayo ina mashiko asilimia 100!***

Sura ya kwanza ya Biblia inaeleza Mungu anaumba binadamu, na sura ya mwisho ya Biblia ya ufunuo 22 yaeleza Mungu anamwalika kila mmoja kunywa maji ya uzima bure kabisa, bila hata kutoa senti. Biblia yaonyesha Mungu anajihusisha mno na mwanadamu na anamfahamu mwanadamu na kujishugulisha na maisha yake ya kila siku. Upendo Wake wa ajabu unanionyeshwa kwa kifo cha Mwana Wake Yesu Kristo msalabani. Kafara hii ya dhambi aliyoifanya inamruhusu kila mmoja wetu kuhesabiwa haki mbele za Mungu kupitia Imani rahisi ya katika Kazi ya YESU. Ukweli unapatikana kwenye Maandiko, ila kwasababu kuna kurasa nyingi tumepita kama wale walio angani na satellite ili tufanye muhtasari wa kushtua ladha yako ili uwe unapitia Kitabu cha Biblia kila siku. Mungu anapenda watu Wake na kuwajali sana ndiyo ujumbe wa Biblia katika kila kitabu. Onja, nawe utaona BWANA ni Mwema!

**Biblia ni ya kutuongoza katika maisha. Soma Biblia kwa mpango na utapata faida Zaidi. Madhumuni yetu binafsi au mahitaji yatatuelekeza. Je, tunataka faraja, au kutajirisha Kesha yetu ya usomaji wa kila siku? Biblia nyingi zina Mistari inayofanana ifuate hiyo. Wengine wamepata faida waliposoma kitabu kimoja cha Biblia kwa mwezi mmoja. Vifaa vya kusoma Biblia ni Biblia yenyewe Ndiyo muhimu, Mafungu yanayofanana, notisi Zake, ramani ya matukio ya Biblia, Jiografia na historia (Abraham Mesopotamia, na Barua za Paulo), concordance kama Ile ya Strong, kamusi ya Biblia, Lexicons, na commentary.**

**Jua maana ya Maneno, jua historia, jua mistari inayofanana na hiyo, soma habari zote zihusianazo na hiyo mada kwenye Biblia. Madhumuni ya kusoma yawe sahihi yaani kuwasiliana na Mungu, kusikia sauti Yake na siyo kupata maarifa peke yake, au kuleta ubishani, wa historia, majina, miji na utamaduni unazosoma humo. Tuombe Roho wa Mungu kwa uongozi atuongoze katika Kweli yote, soma pole pole, ukitafakari kama yule alaye**

**au amunganye kitu kitamu kabisa. Mtu hataishi kwa mkate tu ikimaanisha Neno la Mungu ni muhimu kulila, kulitafuna, kulimeza, kuliyeyusha na ndiyo lilete faida mwilini. Tujiulize tunaposoma, Je? Mungu anazungumza na mimi nini hapa? Uwe mtiifu na tayari kulifuata ili ubadilishwe na kufanana Naye. Baada ya muda Biblia itakuwa mwenzi wetu wa karibu, ikituongoza na ikitubadilisha, Naye Mungu atatuwezesha na kututumia kuibadilisha dunia, na kuongoza wengi kulifuata Neno Lake na kuwa kwenye ufalme wa Mungu siku moja**

Usitoe udhuru kama sisi, tulivyotoa udhuru, japokuwa una uzoefu mdogo na elimu ndogo ya theolojia au ya kuandika kitabu mwombe Mungu Akumwagie Roho Wake na kuleta tofauti kwa kuwapelekea watu Neno, na hata kuwanunulia nakala ya Biblia. Tumeomba wengi waendelee kutuombea ili tuandike vitabu vingine. Imepita mwaka tangu tulipoona hitaji hilo, na tunashukuru Mungu kwa

Twajuaje kwamba Biblia ni Neno la Mungu au la Kweli? Kila mtoto apaswa kujua kujua jinsi ya kujibu hili swali la tumaini tulilo nalo. Kuna sababu nyingi, ila chache tutazieleza ni KAMA IFUATAVYO;

1.Maisha ya Kristo yameathiri historia na nyakati mpaka ikatengwa, kabla ya Kristo KK na Baada ya Kristo BK na yaliyotabiriwa yametokea.

2. Machimbo ya vitu vya kale (akaeolojia) inaafikiana kabisa na matukio na historia ya Biblia. Maandishi ya historia kwenye sehemu za matukio. Mfano kuonekana kwa magurudumu ya magari ya Farao kwenye Bahari ya Shamu n.k -Historia.

3. Mamilioni ya maisha yamebadilishwa na kuwa mbaraka kwa watu kwa ajili ya Neno hili. Hakuna aliyesoma Jiografia na kusema “Baada ya kusoma jiografia, moyo wangu umeamua kuchagua mema”, La! hasha, ni baada tu ya kusoma Neno la Mungu ndiyo watu wamebadilishwa.

Neno la Mungu ni dira na ramani yetu duniani. Neno la Mungu limekuja kwetu kwa kuvuviwa kwa watumishi wa Mungu kama manabii kama Musa aliyekuwa mtoto wa Farao, Luka aliyekuwa tabibu, Daniel aliyekuwa waziri mkuu, Mathayo aliyekuwa mtoza ushuru, Sulemani, Daudi waliokuwa wafalme, Amos aliyekuwa mchungaji wa mifugo na mkulima wa makuyu. Kuvuviwa si kama imla, kwamba waliambiwa waandike Neno kwa Neno, bali mawazo yalivuviwa na wakaandika kwa jinsi walivyoona, mfano wengine waliandika kimashairi, wengine kama visa. Biblia imethibitika kuwa Neno la Mungu. Hakuna kitabu kinachoweza kujibu maswali ya binadamu kama hichi. Hakuna kitabu kinachotuliza shauku na upweke wa mioyo ya watu bali Biblia tu! Ina mambo kwa kila mtu, wa kila umri, na wa kila aina. Ina mwangaza wa maarifa na hekima, maarifa na ufahamu wa kuangaza mafikira yetu na kuyatakasa. Ni ufunuo toka kwa Mungu hai wa mbinguni, wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Mungu amelitunza Neno Lake katika historia, kwa maelfu ya miaka. Zaidi ya mara 2600 waandishi wameandika “BWANA akasema”. Hasa kwenye kitabu cha Walawi. Biblia ina Maagizo, shuhuda, Sheria, na Amri za Mungu.

Biblia ina vitabu 66, 39 vya Agano la Kale na 27 vya agano jipya. Agano la Kale liliandikwa Kiebrania na Agano Jipya kigiriki. Imechukua zaidi ya miaka 1500 kuiandika Biblia bali waandishi wote, wanaokadiriwa kuwa 40 walikuwa na mtiririko wa mada moja (theme), na wala hawakupingana, maana walivuviwa na Mungu mmoja. Biblia yaweza kuwa na takribani ya visa 407 hivi vya watoto. Biblia ina sura 1189. Sura refu kupita zote ni Zaburi 119, na kitabu kirefu ni zaburi hiyo. Sura

fupi kupita zote ni zaburi 117. Zaburi 118 ndiyo sura ya katikati.
Je unakiamini Kitabu cha Biblia, ambacho ni kikuu kuliko vyote (Kitabu cha vitabu). Je unakisoma, na kuacha Ujumbe Wake uzungumze na moyo wako? Utakuwa mtu tofauti ukifanya vile. Anza kukiamini leo kama hakukiamini, na kama unakiamini bila kukitii, anza kukitii leo na kama unakiamini na kukitii endelea kukua ukizaa matunda yapasayo toba. Rafiki yetu mmoja anaitwa John Bradshaw anayetoka New Zealand alituambia alipokuwa akiendesha mji Fulani kule Tennessee aliona nyumba inawaka moto. Akajiwazia moyoni kama watu walio mule ndani walijua hilo. Akasema hapa ni ughaibuni na magharibi hawa watu wanajua nyumba yao inaungua, na nikifika pale na kupiga hodi na watu siwajui watafikiri ni mwenda wazimu. Ila akajipa moyo, na akaendesha gari lake mbele ya ile nyumba na kugonga mlango, hakuna mtu alikuja kufungua, naye akafungua mwenyewe na kuita "jamani nyumba yenu inaungua moto!." Familia ilitoka mle, baba mama na watoto wakishangaa huyu kichaa ametoka wapi, ila alipowaeleza walitimka mbio wakatoka nje na wakati huo Bradshaw alikuwa ameita zima moto, nao wakaja, ila nyumba iliteketea. Ila maisha yaliokolewa! Watu wasiosikia habari za hukumu siku ya mwisho za Mkombozi wataungua moto vile vile, na hawatakuwepo tena milele zote. Je, wewe kwa kuwaonea haya au kuona unawasumbua watu uko tayari waungue tu? Basi waambie habari njema za ufalme na waache wakatae wenyewe. Siku ile vitabu vitafunguliwa na habari za kila mmoja wetu zitawekwa wazi kabisa, habari zote zisizoungamwa. Je, wewe unapenda uovu wako usomwe na kila mtu aujue kweli? Mimi sitaki, nataka niungame uovu wangu saa hii!

Biblia haijakamilika bila Agano la Kale. Agano Jipya ni mwendelezo wa Agano la Kale! Maisha ya Kristo yana maana kutokana unabii wa Agano la Kale. Agano la kale ni kivuli cha Agano jpya. Huduma ya Yesu ingekuwa haileweki bila Agano la Kale. Sheria ya Mungu Mtakatifu zinaonyesha jinsi ambavyo Yesu Asiye na dhambi Ndiye atakuwa Mkombozi. Agano la Kale Ndiyo msingi wa Agano Jipya, bila hilo haliwezi kuwa na miguu (base). Agano Jipya ni Mwendelezo! Mafundisho Makuu yanafundishwa katika Agano la Kale. Jipya linatafsri la Kale. Ni mkate wa Uzima na chakula kwa Muumini.
Ili tupate Biblia yetu mengi yalitokea, hizi hazikuwa enzi za kalamu na makaratasi! Pia Watu wengi wamelifia Neno hili ili kutuwezesha tulipate. Vitabu vya Musa vyaweza kugawanywa kutoka mwanzo kwa jinsi hii-- vitabu vya Musa vitano(5), vitabu vya historia (12), vitabu vya mashairi vinne (4), vitabu vya manabii vikubwa vitano (5), na vidogo na vikubwa kumi na tatu (13), vitabu vya injili vinne(4), kitabu cha matendo na historia ya matendo ya mitume kimoja(1), barua za Paulo kumi na vinne(14), na barua za mitume wengine(7), na mwisho kitabu cha unabii cha ufunuo(1).
Musa aliandika vitabu vitano vya mwanzo wa biblia akiwa Midiani, na kitabu cha Ayubu ndicho cha zamani kupita vyote na yasemekana alikiandika kabla ya vile vitano vya torati. Kutokana na Biblia dunia yetu ina miaka kama 6000 hivi. Gharika ilitokea mwaka 2348 BC na kuzaliwa kwa Yesu ilikuwa miaka ya 4 KK - 1 BK. Biblia inaeleza wazi wazi kwenye ufunuo 12 kwamba kulikuwa na vita mbinguni na Shetani alitupwa mbinguni kuja hapa duniani na kuwadanganya wazazi wetu Adam na Hawa kuasi. Hapo ndipo dhambi ilipoingia duniani. Dhambi ni uasi wa Sheria za Mungu. Tukiungama na kuwa na toba ya Kweli, Mungu ni mwaminifu,

anatusamehe na tunaanza maisha mapya. Pambano kati ya uovu na wema, au shetani na Mungu linaendelea mpaka siku ile ya mwisho ambapo Kristo atakuja na Mungu Atafuta machozi ya watu, kutakuwa hakuna tena kilio, huzuni wala kifo. Wale walioshinda kwa neema za Mungu, wakimtegemea, wakimtii na kumtumaini Yeye watapata zawadi ya uzima wa milele mbinguni(Paradiso). Hiyo ni zawadi kubwa kupita zote duniani. Mpendwa msomaji, mtumaini Bwana na kumchagua kila siku katika maisha yako. Mambo matano muhimu kwa kila binadamu ni kwanza kumjua Mungu na kufuata njia Yake, pili, kuomba kila siku, tatu, kusoma Neno Lake kila siku, nne, kuabudu kwenye ushirika na wengine, na tano kushuhudia matendo makuu ya Bwana kwa wengine.

Agano la Kale liliandikwa Kiebrania kwenye makaratasi marefu ya papyrus au sufu. Yalitafsiriwa baadaye kwa kigiriki, yakaitwa "Septugiant" kwa vile Wayahudi wasomi 70 wa Theolojia walishugulikia na tafsri Yake 285 A.D. Isipokuwa sura chache za Danieli ziliandikwa katika kikaldayo. Agano jipya liliandikwa Kigiriki. Baadaye maagano haya mawili yalitafsiriwa kwa kilatini. Lugha hii ni ya zamani, na haizungumzwi leo hata enzi zile haikujulikana na wengi isipokuwa wasomi. 1380 John Wyclife aliitafsiri kingereza. Kutafsiri Biblia siku hizo kilikuwa kitu cha hatari kwani utawala wa kanisa ulikataa mtu wa kawaida (mlei au-lay) kuwa na Biblia. Martin Luther wa Ujerumani katika wakati ule wa matengenezo aliitafsiri kijerumani, alisema "Kwanini Neno la Mungu limefungiwa kwenye lugha zilizokufa? (hazitumiki). Wengine kama Tyndale walisaidia kufanya Biblia ziwe mikononi mwa watu. Wengi waaminifu wameuwawa wakishugulika usiku na mchana ili mtu wa kawaida awe na Biblia. Siku zile watu walinakili kwa mikono, na walipogusa Biblia zao machozi yaliwatoka, maana walijua wanagusa kitu cha thamani kuliko vyote duniani. Hatimaye ulifika wakati wa uhuru na vyama vya Biblia vya Uingereza na Marekani vilianza kuchapicsha Biblia nyingi (English and American Bible societies). Vyama hivi vimesaidia hata kwetu Afrika mashariki kutafsiri Biblia ya Kiswahili ili watu wasome Neno la Mungu. Mpendwa msomaji, fanya hima uwe na Nakala yako ya Biblia. Mwombe Mungu atakusaidia upate Nakala ya Neno Lake, maana ni Mweza wa Yote. Je unayo nakala ya Biblia hapo ulipo? Ishike, itazame vizuri. Umeshika kitu cha thamani kuliko pesa, dhahabu, almasi, au tanzanite. Maana mbingu na dunia na vitu vyote vitapita ila NENO la Mungu ni la milele, hili ndiyo pasipoti yako ya maisha bora zaidi na pasipoti ya kwenda mbinguni, kwani ukilisoma, ukalipenda, na kulitafakari, na kulitenda, wewe una uzima wa milele. Milele ni Zaidi ya miaka Trilioni moja, ni muda mreeeeefu sana usioisha.

Biblia ndiyo kitabu cha kwanza kuchapishwa mwaka 1456 AD na mashine ya kuchapa aliyoitengeneza Johannes Gutenberg, kule Ujerumani. Kabla ya hapo japo watu walisema uchapaji na utengenezaji wa makaratasi ulianza miaka maelfu kule China, ila watu walinakili Biblia kwa mikono. Kusudi la Gutenberg kutengeneza mashine ya kuchapa ni ili aichape Biblia ya Kijerumani. Biblia ndiyo bado ndiyo kitabu kinachouzika sana kuliko vyote ulimwenguni. Biblia imetafsiriwa kuliko kitabu kingine duniani. Kitabu hiki kimebadilisha maisha ya watu waovu wakawa watu wema. Hakuna aliyewahi kusema "Nilikuwa mwizi na sasa ni mtu mwema kwa kusoma hesabu au kemia!". Au sasa nimeona njia ya kwenda mbinguni kwa kusoma uhasibu au uanasheria. Mbali na kwamba yote yaliyotaribiriwa kwenye Biblia yametokea (mamia ya unabii, kuna mengine mengi yanayofanya kiwe Kitabu cha Mungu na cha Pekee). Ni Neno la Mungu tu, Ndiyo linabadilisha

maisha yetu na kutufanya tuwe viumbe bora kimwili, kiakili na kitabia. Wengi ambao wamelisoma wamesema "sijapata kuona uzuri na utamu kama huu". Biblia itazidi kung'aa na kuwa dhahabu kwa thamani kila siku unapoendelea kuisoma. Utamu Wake utakuwa wa ajabu, na wala hutapenda uache kuisoma! Wengi waliokuwa na uwezo mdogo darasani wamefanya vizuri kwa kulisoma Neno hili kwani linaboresha akili. Hakuna kile kinachopanua ubongo lishe na nishati kama Neno la Mungu. Watu wamejua ya mbeleni (future) kwa kulisoma na wamejitayarisha kwa matukio ambayo wasingeweza kujua kwasababu ya kusoma Neno la Mungu.
Binadamu wote tumepotoka na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, na mshahara wa dhambi ni mauti. Bali Mungu ametoa njia kupitia Kafara ya Mwana Wake Kristo. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda Ulimwengu, ili kila amwaminiaye asipotee, bali apate uzima wa milele. Mwanadamu hakuja ili ahukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe na Yeye Yohana 3:16-17. Mpendwa msomaji, tuna matumaini sote ya kwenda kuishi mbinguni milele na milele na Baba yetu wa mbinguni. Hebu tupige moyo konde, tumwombe atusaidie katika safari hii na tupate marafiki wazuri wasio na misukumo ya uovu, ili tushinde mbio hizi.
Miaka 170 iliyopita kule Ulaya walitokea watu wa nadharia potofu za uibukaji wa mwanadamu kutoka minyoo, chura, nyani na kisha binadamu. Hakuna aliyesikia redioni "leo tunakaribisha raia wapya toka msituni Gombwe au Virunga, wamebadilika toka sokwe au gorila kujiunga nasi!". Hizi ni nadharia potovu, ovu na za uongo. Uibukaji si sayansi, ni dini, kwani haifuati vigezo vile vitano vya sayansi yaani kuangalia, kupatwa na maswali, kufanya uchunguzi, kukusanya habari au data, na kuhitimisha-( observation, hypothesis, experiment, data, na conclusion ). Darwin baba wa dini ya ukafiri (uibukaji) alisomea theolojia tu, na wala hakusomea sayansi na wala hakuwa na shahada ya sayansi, yeye alifanya madarasa machache ya elimu ya mimea. Aliingia kwenye meli ya Uingereza akiwa amepewa lifti ya meli MS Beagle kuangalia mambo aliyosema kuelekea Galapagos America ya kusini mwaka wa 1845, na vitabu viwili, Biblia na kitabu cha Lyle. Tujihadhari na watu ambao hawajali Mwumbaji wala uumbaji Wake. Sisi tumeumbwa na Mwenyezi Mungu au nguvu kubwa zaidi yao kwa makusudi makubwa. Ila kila utamaduni una dhambi zake, kila kabisa au jamii ina dhambi zake! Na ndiyo maana sote binadamu tunamhitaji Yesu, Hatuko salama, kabisa, hakuna hata mmoja yuko sawa! Tumeoza sote, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Tu wadhambi tunaohitaji msaada! Mungu Mwenye uwezo wote alikosa njia nyingine ya kutukomboa, isipokuwa kumtuma Yesu, basi hiyo tu itujulishe dhambi ni kitu cha kutisha na kilihitaji ufumbuzi wa dharura na mzito!
Kuna wengine wana Biblia yenye vitabu vinavyoita Apokrifa, navyo ni kama Makabayo, Tobiti, Yudithi na maongezo ya vitabu vya Esta au Danieli. Hivi vitabu ni vizuri kwa historia na si vya kuvuviwa kwani vinapingana na Kanon/Canon (Maandiko) na kanuni za Neno la Mungu ni kama vile vya mapokeo ya kiyahudi kama Talmud. Vitabu vingine vimepotea kama cha Iddo, Nathan, barua kwa Laodikia, 3 Wakorintho na vingine. Hivi waliandika watu wa Mungu waliovuviwa na vimetajwa. Cha kukumbuka ni kwamba, vile tulivyo navyo 66 ni tosha kutufikisha mbinguni kwa Baba yetu. Haleluya, Maranatha.
Biblia si ushauri bora au maoni, bali sauti ya Mungu. Wazungu wanasema "The Bible says it I believe it, and that settles it." Yaani kitabu cha Neno la Mungu Biblia kikisema, basi nakiamini, na hiyo inatoa mashaka yangu yote. Soma Neno la

Mungu, liamini, litafakari, likariri, na liishi, hii ndiyo dira yetu safarini duniani.
Tuisomaje? Wasomaji Wengi wapya wanasema hawajui waanzaje. Kuna njia nyingi za kuisoma. Wengine wameanza Mwanzo na kukwama walipofikia Walawi kwa zile taratibu za Kafara. Japo Walawi 16 ni kitovu cha Ukombozi wa mwanadamu kwenye Agano la Kale! Tunashauri kuanza vitabu vya injili kama Marko, Mathayo, Luka na Yohana. Kisha Matendo na kurudi kitabu cha Mwanzo na Kutoka na kufuata huo mtiririko. Waweza kuisoma kwa kuchukua mtu mmoja na maisha yake. Waweza kuinakili au kuifanyia muhstasari, kama sasa tunavyofanya ambayo imenifungua macho kwa njia nisiyoweza kuileza. Na bado nina mapungufu mengi! Waweza kuisoma na kamusi kutokana na mada/topiki. Utakapoizoea utaweza kirahisi kuanza mwanzo mpaka mwisho kama wengine wetu tunavyofanya kila siku tunasoma na kusogea mbele tukiomba msaada wa kuielewa. Hata ukisoma mafungu machache kila siku, na kuyafanyia uchunguzi na utafiti wa kina (study) yanatosha, kuliko mengi ambayo unashindwa kuelewa maana yake. Maana si kusoma tu, ila kulinganisha mistari inayohusu ulichosoma kwenye Biblia nzima. Kabla ya kuhitimisha jambo, ni vyema uonge jambo hilo limezungumziwa wapi, na mara ngapi kwenye Maandiko. Zungumza na wengine wanavyoisoma, ila isome kwa furaha na ***kuomba kabla hujaanza***, usijipangie kusoma kurasa nyingi ukaona ni adhabu na Pengine usielewe unachosoma. Kusoma Bibla inachukua masaa kama 70 au 80 tu. Na wiki moja ina masaa 168 hivyo waweza kuimaliza kusoma kwa wiki tu! Ila wahitaji muda wa kucheua na kutafakari hata fungu moja tu, utashangaa utakayoyapata! Mfano Danieli 8:14 “Akamwambia, Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa.” Hili linaweza kukuchukua miezi kulitafakari na kulielewa, na linahusiana na mamia ya Mafungu mengine kwenye Biblia! Ukiwa na muda tuandikie tukueleze kile sisi tulichogundua, nawe utatuelezea kile ulichogundua! Usifanye kwa kasi na presha au msukumo usio na furaha! Biblia ina Ujumbe kwa kila aina ya mtu, mzee, kijana,msomi, mtu wa kawaida, tajiri, masikini, mfupi, mrefu, mweusi, mweupe.
Ni matumaini yetu kwamba utakuwa mfuasi wa Mwenyezi Mungu na kuleta wengi Kwake. Usikite kwenye mabishano na watu bali kuwaambia maandiko kwa upendo (shiriki-share). Maana waweza kushinda mabishano au pambano, ila ukapoteza roho ya thamani au ukashindwa vita. Unaweza kushinda kwenye mabishano ila ukapoteza roho. (you might win argument but loose precious soul).
**Biblia ni ya kutuongoza katika maisha. Soma Biblia kwa mpango na utapata faida Zaidi. Madhumuni yetu binafsi au mahitaji yatatuelekeza zaidi. Je, tunataka faraja, au kutajirisha Kesha yetu ya usomaji wa kila siku? Biblia nyingi ina mistari inayofanana ifuate hiyo. Wengine wamepata faida waliposoma kitabu kimoja cha Biblia kwa mwezi mmoja. Vifaa vya kusoma Biblia ni Biblia yenyewe Ndiyo muhimu, mafungu yanayofanana, notisi zake, ramani ya matukio ya Biblia, Jiografia and historia (Mfano ramani wakati Abraham akiwa Mesopotamia, ramani wakati Wanaisraeli wakiirithi Kanani, ramani wakati Yesu anafanya utume, ramani wakati wa barua na safari za Paulo), kamusi ya Biblia.**
**Jua maana ya Maneno, jua historia, jua mistari inayofanana na hiyo, soma habari zote zihusianazo na hiyo mada kwenye Biblia. Madhumuni ya kusoma yawe mema yaani kuwasiliana na Mungu, kusikia sauti Yake na siyo kupata maarifa peke yake, au kuleta ushindani/mabishano kuhusu**

**utamaduni, majina ya miji nk. Omba Roho wa Mungu kwa uongozi ili atuongoze sote katika Kweli yote, soma pole pole, ukitafakari na kuakisi. Mtu hataishi kwa mkate tu ikimaanisha Neno la Mungu ni muhimu kulila, kulitafuna, kulimeza na ndiyo litaleta faida mwilini. Tujiulize tunaposoma, Je? Mungu anazungumza na mimi nini hapa? Tuwe watiifu na tayari kulifuata ili tubadilishwe na kufanana Naye. Baada ya muda itakuwa mwenzi wetu wa karibu, ikituongoza na tutabadilishwa na kuwezeshwa na Mungu, Naye atatutumia kubadilisha dunia au kuipindua dunia juu chini, na kuongoza wengi kulifuata Neno Lake, kubariki watu wengi na kuwa kwenye ufalme wa Mungu siku moja, Tuombeane sana, Mwisho u Karibu sana, dalili zinatuambia na tunaziona!**

## ***BIBLIA NI RAMANI***

***Biblia imezungumza, nami Ninaamini, na tatizo linaisha.***

*Kitabu hiki kimebeba fikra ya Mungu, Hali ya mwanadamu, Njia ya wokovu, Hatima ya wadhambi, na furaha ya wenye haki. Mafundisho Yake ni Matakatifu, kanuni Yake zadumu milele, historia Yake ni ya Kweli na Suluhisho Lake ni la kuaminika, Kisome upate hekima, kiamini ili uwe salama na kijaribu ili uwe Mtakatifu.*

*Kina nuru ya kukuongoza, chakula cha kukuwezesha kuboreshwa, na faraja itakayokujaza furaha. Ni ramani kwa msafiri, Fimbo kwa mahujaji, dira ya rubani, upanga wa askari, na Mkataba kwa Mkristo. Hapa Paradiso hurejeshwa, Mbingu hufunuliwa, na milango ya kuzimu hufungwa. Kristo Ndiye muhusika Mkuu: Wema wetu, muundo Wetu, utukufu wa Mungu, na mwisho na Mwanzo yaani Alfa na Omega. Kitabu hiki hakina budi kujaza akili, kutawala moyo, na kuongoza mapito yetu.*

*Kisome taratibu, mara kwa mara na kwa maombi. Ni madini ya utajiri, paradiso ya utukufu na mto wa furaha. Kimetolewa kwako maishani, kitafunguliwa wakati wa hukumu, na daima kitakumbukwa milele. Kinatoa kiwango cha juu cha uwajibikaji, Kitatoa ujira kwa kila mtenda kazi bora na kitawahukumu wote waliochezea mambo Matakatifu. Kamwe hakuna kitabu kingine kinachoinua akili na kuongeza uwezo wa kufikiri kama Biblia.*

*Iamini upate hekima, isome uwe salama, Ijaribu uwe mtakatifu. Biblia si kitabu cha kukupatia taarifa bali kitabu cha kukubadilisha. Ni Sauti ya Mungu ikizungumza, tena ni sauti Yenye Mamlaka kuu Mbinguni na Duniani na galaksi zote. Bwana amelikuza Neno Lake juu ya Jina Lake. Mbingu na nchi zitapita lakini si Biblia. Biblia imeshinda kila aina ya changamoto za nyakati zote.*

Kamwe "Usiogope, kwa maana Mimi ni pamoja nawe, usifadhaike, kwa maana Mimi ni Mungu wako, Naam, Nitakutia nguvu, naam nitakusaiidia, nitakushika, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki Yangu" Isaya 41:10. Kweli "macho hayajaona, wala masikio kusikia wala kuingia katika mawazo ya Mwanadamu yale ambayo Mungu ametutayarishia wanadamu!". Hebu tusome Neno Lake ili tuzijue ahadi 3500+ na kuzidai. Inachukua muda wa masaa 70 tu hivi kusoma Biblia, watu wamemaliza kusoma Vitabu vikubwa zaidi. Nilipoenda kwenye shule ya matabibu Loma Linda California ili niweze kuchukua madarasa ya tiba, nilikuta mavitabu makubwa sana miaka hiyo ya tisini, mengine yalikuwa dola 2000 kwa kimoja tu! Niliishangaa watu waliyasoma, na wakayamaliza na kuyafanyia mitihani. Biblia ni kama dola nane tu hivi kununua na kurasa kama 1000 tu. Hatushauri usome kwa haraka, bali sura moja mpaka tatu kwa siku. Na kama una kamusi yenye maelekezo ya Biblia (concordance) waweza kuitumia ila maombi na mafunuo toka kwa Bwana ni kipaumbele kwa ufanunuzi wa watu. Biblia isisomwe bila ya kusali. Hichi si kitabu cha kawaida. Ni kitabu cha mbingu, na kukielewa chahitaji Mwenye Kitabu atusaidie. Piga magoti ukiweza, omba kupewa uwezo wa kukielewa na kufanya yale unayoyasoma. Dai ahadi zile unasoma siku ile, na mwulize Mungu 'Je wataka nielewe nini katika yale ambayo nimesoma leo? Na Naomba unisaidie niweze kuyatumia katika maisha yangu ya kila siku hasa leo'.

Biblia ni ramani, taa na maktaba. Yawezaje kitabu kimoja kikawa na vitu vyote

hivi? Biblia ni ramani kwa vile inatuonyesha njia salama, na kwamba tukikaa katika njia hii tuna uhakika kwa kufika kwa Yesu aliye upande usioshindwa dhidhi ya Shetani, adui yetu. Yesu ni njia hii. Biblia ni mwanga wa njia yetu, iking'aa na kung'aa kwenye ile njia iendayo uzimani. Adui alijaribu kuizima ile taa, ila mwanga wake umekuwa zaidi kutuonyesha ile njia salama. Angalia Biblia yako na isome, usitumie muda wako sana kusoma vitabu vya binadamu hasa wale wasiompenda Mungu (makafiri) itakuondolea ladha ya Biblia. Hakuna mtu katika kutambua noti bandia anatumia noti feki bali noti ile halali. Watu wengi wamechukua muda kusomea miungu ya ugiriki, na urumi na miungu mingine ya tamaduni mbali mbali. Usipoteze muda, chukua muda kusoma habari za Mungu wa mbinguni. Mungu wa Ibrahimu, Isaka, Yakobo na Yusufu.

Biblia yahusu watu, sehemu, na mambo yaliyotokea zamani, leo na hata siku za mbeleni. Vitabu vyote vyatuonyesha pambano kati ya shetani na MUNGU linaendelea. Na kila binadamu anachagua upande kila kukicha anaotaka kuwa. Kutochagua ni kuchagua. Watu, vitu na sehemu za Biblia zinatuonyesha mapambano haya zikitupa maonyo ili kwa saburi na faraja tuchague upande ulio salama, upande wa Mungu. Vitabu vya Agano la Kale viliandikwa Kabla ya Kristo kuzaliwa duniani, na vitabu vya Agano Jipya viliandikwa baada ya Yesu kufa na kufufuka. vitabu vyote ni muhimu na vinasaidiana kutuongoa tujue kila tunachopaswa kujua kuhusu Mungu na mpango Wake wa wokovu, Vinatusaidia sana tufanane Naye. Uchaguzi wetu unapelekea Hatima yetu! Kwanini tusome Biblia kila siku? Toa sababu zako Nne! Kila asomaye hujifunza kumtumaini na kumtegemea Mungu, na kujua Mungu afanya kila kitu kutuokoa na ujanja wa ibilisi katika kutuangamiza. Zaburi 119:9-11.

***Kuna Sababu zaidi ya 100 za Kuisoma Biblia, nitaandika chache tu!***

1. Ni Jinsi Mungu Anavyoifunua Tabia Yake, na kutuunganisha na MUNGU -Kutoka 34:6-7, Waebrania 1:1-3
2. Inatoa Maagizo kwa Maisha ya Kila Siku na kunilinda- 2 Timotheo 3:16,17, Zaburi 32:8
3. Inanifundisha Jinsi ya Kuomba-Luka 11:1-4
4. Inaeleza Jinsi ya kupata wokovu wa kila mwanadamu-Yohana 3:16
5. Inaeleza Jinsi ya Kushiriki Injili-Mathayo 28:19-20
6. Inakufundisha Jinsi ya Kumtumaini Mungu -Mithali 3:5-6
7. Inaonyesha Mapenzi ya Mungu Yalivyo, na kufanywa nia zetu upya- Warumi 12:1, 2
8. Imejaa Ahadi naBaraka za Mungu, na hivyo itakubariki!- Kumbukumbu la Torati 31:8
9. Ni Historia sahihi ya mwanadamu na kila kilichomo duniani-Waefeso 4:31-32, Zaburi 78:3-4
10. Inakufundisha Jinsi ya Kusamehe- Waefeso 4:31-32
11. Kusoma Biblia hutuwezesha kuwa na uhakika wa yale ambayo Mungu alisema. Biblia ndiyo mamlaka yetu ya mwisho. Ndiyo Ukweli wa mwisho -Yohana 17:17
12. Inauliza na Kujibu Maswali Makuu Tumetoka wapi? Kwa nini tuko hapa? Tunaenda wapi? Inamaanisha nini kuwa mtu mzuri?— Zaburi 10:1
13. Inakuboreshea utamaduni wako, mfano lugha yako isiwe na matusi, usile watu, mavazi, usafi wa moyo, kuachana na uchwai- Mhubiri 1:9

14. Inafunua Jinsi Mungu Anavyotupenda - 1 Yohana 4:7-8
15. Inatupa uzima wa milele (mbinguni) -Yohana 17:3
16. Husaidia kuishinda na kuikimbia dhambi na kutakaswa dhambi Zaburi -110:9,10,11 na Yohana 15:3
17. Inaniondolea msongo wa mawazo -1 Samweli 30:6-8
18. Hutufundisha kumwiga Mungu ambaye Yeye ni Upendo - Waefeso 5:1
19. Hutuwezesha kupokea matamanio ya mioyo yetu Yohana 5:39-40
20. Hutusaidia kuzaa matunda-Zaburi 1:2-3
21. Hutupatia ujasiri-Yoshua 1:8-9
22. Ni chakula chetu-Mathayo 4:4, Yohana 6:63
23. Inafanya niwe mwenye rehema na upendo kwa wengine-Marko 12:30-31
24. Inakulinda na Mafundisho ya Uongo na hivyo utamwabudu Mungu katika Roho na Kweli - Yohana 4:1
25. Inakuhimiza Kutumia Muda Wako kwa Hekima - Waefeso 5:15-16
26. Mungu anakupa mwongozo, kwani Yeye Ndiye Njia, Kweli na Uzima - Zaburi 119:105, Yohana 14:6
27. Hukusaidia Kuepuka Majaribu kwa maana ni silaha na kinga ya kukuhifadhi kutokana na uraibu- Waefeso 6:11.
28. Ni HAI!- Yohana 7:38
29. Itakupa Uhuru -Warumi 8:17
30. Kwa Uponyaji, kuburudishwa na kudumisha, kimwili, kiroho, kiakili, kijamii na kiuchumi-1 Petro 2:24, Mathayo 4:4
31. Inanisaidia kutatua matatizo yote-Yakobo 1:5
32. Itakusaidia kukumbwa na bubujiko la furaha na amani ipitayo akili.

**<u>Mambo mane ya Biblia</u>**

1. Hakuna kitabu kinachopendwa na watu wapo tayari kufa kwaajili yake
2. Hakuna kitabu kinachochukiwa kama hiki na watu wengi wametaka kukiangamiza
3. Hakuna kitabu ambacho watu wengi wanacho kama hiki na hawakisomi
4. Hakuna kitabu ambacho watu wengi wanasema wanakiamini, bali hawajui hata mambo machache yahusianayo nacho
(many people believe it but know hardly anything about it).
Je, wewe upo kundi gani kati ya haya mane?

**<u>Vitabu vya Biblia vimegawanyika katika makundi kumi:</u>**

1.Vitabu vitano vya Musa (Pentateuch) :
Mwanzo, Kutoka, Walawi, Hesabu, na KumbuKumbu la torati,
2.Vitabu vya Historia :Joshua, Waamuzi, Ruth, 1 Samweli, 2 Samweli, 1 Wafalme, 2 Wafalme, 1 Mambo ya Nyakati, 2 Mambo ya Nyakati, Ezra, Nehemia, Esta, na Ayubu (Yumkini iliandikwa na Musa).
3. Vitabu vya mashairi: Zaburi, Mithali, Mhubiri na wimbo ulio bora au Wimbo wa Sulemani.
4. Manabii wakubwa vitabu vyao ni virefu: Isaya, Yeremia, Ezekiel na Daniel.
5. Manabii wadogo, vitabu vyao ni vifupi: Hosea, Yoeli, Amosi, Obadia, Yona, Mika, Nahumu, Habakuki, Zefania, Hagai, Zekaria, Malaki.
6. Vitabu vya Injili: Mathayo, Marko, Luka, Yohana.
7. Kitabu cha Historia Agano Jipya: Matendo.

8. Barua za Paulo: Warumi, 1 Wakorintho, 2 Wakorintho, Wagalatia, Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, 1 Wathesaloniki, 2 Wathesaloniki, 1 Timotheo, 2 Timotheo, Tito, Filemoni, Waebrania.
9. Nyaraka zingine: Yakobo, 1 Petro, 2 Petro, 1 Yohana, 2 Yohana, 3 Yohana, Yuda.
10. Unabii: Ufunuo, Daniel

Kwanini Mungu alitupatia Biblia? Makusudi ni ili tumjue Yeye aliye Muumba na Mkombozi wetu na kuelewa njia Zake. Hapo Mwanzo Mungu alipoumba alizungumza na Adamu na Hawa moja kwa moja, ila baada ya dhambi tumekuwa na kiwambaza na hivyo kuhitaji manabii (watu wanaozungumza kwa niaba ya Mungu). Dini ya Kikristo haimrusu mtu kufanya atakavyo. Muumini apaswa kujisalimisha kwa Mungu, na kuishi kutokana na Maandiko au NENO litokalo kinywani mwa BWANA. Muumini apaswa kuwa mtiifu na anayempenda Mungu kwa moyo wake wote, roho yake yote, nguvu zake zote na akili zake zote na jirani kama nafsi. Upendo ni jambo muhimu mno na fumbo na siri ya ajabu! Ukatili kwa wengine au kutenda kwa hiana kwa watu au kwa Mungu ni dhambi. Mungu alizungumza na watu uso kwa uso kabla ya dhambi pale Edeni, ila ametumia Maandiko kuzungumza nasi leo baada ya maanguko ya mwanadamu. Biblia ni sauti ya Mungu ila imeandikwa kwa maneno ya binadamu. Haikuwa imla. Watu wa Mungu waliambiwa ujumbe na kupewa uhuru wa jinsi ya kuuandika. Vitabu vya injili ni mfano mzuri. Vyote vine (4) vimeandikwa kuhusu Masihi, ila vina mawani au ladha yenye shauku (interest), haiba, theolojia na historia ya mwandishi. Biblia ni Neno la Mungu. Biblia ni Neno la Kiyunani likimaanisha "Maktaba". Biblia ni maktaba ya vitabu 66. Wanadamu walivuviwa kuandika. Biblia si imla, ila Maneno yaliyovuviwa na Mungu. Kisha watu waliambiwa wayaandike na wakayandika. Biblia imeandikwa kwa muda wa miaka 1500 hivi, na watu 40 tofauti. Agano la Kale mpaka jipya ni miaka 400. Biblia Ina sura 1189. Biblia iliandikwa kwa lugha ya Kiebrania na Kigiriki. Biblia ina zaidi ya ahadi 3500 kwa mwanadamu, tuzijue ili tuzidai! Mara 365 Biblia imesema "usiogope!". Neno la Mungu ni mamlaka ya mwisho duniani na mbinguni, na lina ujumbe kwa kila aina ya mtu. Lisome, litafakari, lipende, litende, litangaze. Biblia itakupa maana katika malengo ya maisha yako. Kamwe hatujisikia kama mtu duni, au hafifu, maana utajua thamani yako jinsi ilivyo, thamani halisi aliyokutunukia Mwumbaji wako alipokuumba. Utaishi maisha ya madhumuni na maana na kujua katika yote Warumi 8:28 na mwishowe utapewa kutokufa, yaani uzima wa milele. Haijalishi utazeeka, kwani uzee wako utakuwa na tumaini na furaha, kwa kuyaona yale ya mbeleni.
Vitabu vya kwanza vitano na Ayubu viliandikwa na Nabii Musa miaka ya Miaka ya 1500 BC na kitabu cha Mwisho kiliandikwa na Yohana miaka ya 100 A.D. Kitabu tulichoandika cha Nipe Biblia ni muhtasari wa Biblia kwa kuanzia kitabu cha Mwanzo mpaka Ufunuo kama kesha la siku 365. Biblia ina takribani kama wanawake 182 na wanaume 1188.
Biblia inatueleza Historia ya Binadamu toka kuumbwa na Mungu, mpaka kuanguka na kuasi sheria za Mungu pale Bustani ya Edeni kisha ufumbuzi. Katika ufunuo 12 Tunaelezwa kwamba, Shetani aliishi mbinguni na kuwa mwasi wa kwanza. Aliwashawishi theluthi ya malaika wote na kutupwa nao hapa duniani. Hiyo ikawa mwanzo wa pambano kati ya Mungu na Shetani, au wema na ubaya. Vita hii siyo kupigana na bunduki, makombora au mapanga, maana kupigana kwetu si kwa

nyama na damu, na Masihi alimwambia Petro aweke upanga wake alani asipigane. Kupigana na kwa Neno la Mungu (Efeso 6). Kwa sasa tumo katika pambano hili, kitabu cha Ayubu, Isaya 14 na Ezekieli 28 vinatupa picha ya pambano kwa udogo tu. Kuna siku pambano hili litakwisha. Kutokana na Biblia, ishara za nyakati za Daniel sura mbili, saba, nane na tisa ni kalenda tosha ya unabii, yaonyesha tuko wapi, kila mtu asome. Mungu atakuja kuhukumu ulimwengu, na kutoa thawabu kwa wale waliotenda mema kwa neema Yake, tuzo la Uzima wa milele, na kwa wale waliotenda uovu, adhabu. Kila mtu asome sura hizo za Daniel na kujua maana yake ni nini Leo. Mwanzo 1 & 2 ni uumbaji, Mwanzo 3 ni kuanguka kwa binadamu, Biblia yote iliyosalia baada ya hapo ni ukarabati wa dhambi ili isiinue pembe yake asilani- Nahum 1:9, mpaka kufikia ufunuo 19 ambapo hukumu itawekwa, na watu watapewa uzima wa milele na Ufunuo 22 kuishi milele na Mungu, uso kwa uso maisha yasiyo na kikomo. Hakutakuwa na huzuni, vilio, kifo, wala magonjwa. Mimi na wewe mtoto, kijana, dada, kaka, baba, shangazi, mjomba, mama na binamu, tumo kwenye pambano hili zito. Hata mtoto wa miezi anapata shida kujikana nafsi na kutaka yote yaende anavyopenda. Mapambano yote yapo kichwani na moyoni, tunasikia sauti mbili. Twapaswa tuvae silaha za Mungu na kukaa dede, tukikesha na kuomba ili tusiingie kwenye mtego wa hila za mwovu. Kila siku tunamchagua mwenyezi Mungu au shetani Efeso 6 na 2 Korintho 10:5. Wote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, bali Mungu anatusamehe tunapoomba msamaha na kuwa na toba ya kweli. Hila zote, iwe kiburi, hasira, wivu, chuki, tamaa, kutosamehe, mawazo machafu, kudharau watu, unafiki, na hata tamaa zote za macho na mwili na kiburi cha maisha haya, za Wagalatia 5 hebu na zipitwe na wakati. Nasi tuzae tunda la Roho ambalo Mungu Anatusaidia kuishi maisha mapya kwa neema Yake. Ombi letu kuu ni tujazwe na Roho Wake Mtakatifu, tumpende Yeye kwa roho zetu zote, nguvu zetu zote, akili zetu zote na mioyo yetu yote. Na tupate uchungu sana tukiona mtu anapotea, tuone kama mpendwa wetu wa karibu amepotea, na kujaribu kumfikia ili sote tuwe ndani Yake, Naye ndani yetu yaani Yeye mzabibu wa Kweli. Yapaswa tujitoe kikamilifu ili Yeye atupe njozi, misheni, usongo na nyenzo (vision, mission, passion and provision).

Kitabu cha Mwanzo moja mpaka tatu kinyume chake ni Ufunuo tatu mpaka ishirini (reverse). Shetani alitaka sura ya Mungu au mfano wa Mungu kupotea kutoka kwa mwanadamu na kuwa kama hayawani au mnyama tu. Ila Yesu alikuja kurudisha ile sura, na hapa shetani alifurahi kwamba amemfanya Mungu kushuka na kupata mateso, na akajaribu sana toka utoto misheni au utume huo ushindwe, Mungu ashukuriwe kwamba misheni ilifanikiwa kwa ushindi mkubwa kwa kutupatanisha na kuhesabiwa haki kupitia Kwake. Mungu toka Edeni amekuwa daima akijaribu kutufikia wanadamu ili tupate wokovu na kurudisha mahusiano nasi mpaka Ufunuo 19. Ukamilifu wa mbinguni ulifeli kwa Shetani kuasi kule mbinguni, na ukamilifu wa binadamu ulifeli kule Edeni kwa kujifanyia alivyotaka, leo sisi tunapokea zawadi au neema ya Mungu kupitia kwa Imani na kupokea moyo mpya, mtazamo na akili, maisha haya mapya yanaitwa kutembea na Mungu tunazaliwa upya kwenye familia ya Mungu (waongofu) na kisha wanafunzi wa Yesu na mwishowe mitume kuwaambia wengine habari njema.

Biblia imechomwa au kuharibiwa mara nyingi, kuanzia wakati wa nabii Yeremia (Yeremia 36 & 38), watu wameizika nayo ikafufuka, watu wamezifuta nyayo zake, na kuzipotosha kwa kufanya vidole vielekee nyuma na kisigino mbele ila hawakufua

dafu. Tyndale, John Huss, Stefano na wengine wengi mpaka leo wanaendelea kulifia Neno hili kwani kuna watu huchukia wosia wa Neno la Mungu na kuwaua watumishia au hulichoma hili Neno. Siri ya uzima wa Milele inatoka kwa kulijua Neno la Mungu na kulitekeleza kwa neema Yake Bwana- Yohana 17:3 " Na uzima wa Milele ndiyo huu, wakujue Wewe Mungu wa pekee na Yesu Kristo uliyemtuma". Uzima wa milele si kuishi miaka mingi, bali ni kumjua Mwenyezi Mungu!
Twarudia kuwa mamilioni ya watu wamelifia Neno la Mungu ili kuweza kuliweka mikononi mwetu leo. Lisome, liamini, litafakari, likariri, lipende na litende. Tumwamini Mungu tuthibitike, na tuamini mitume Wake ili tufanikiwe. Hakuna kinachotoa furaha kama Neno Lake. Watu wa aina mbali mbali waliandika Biblia; mfano manabii kama Musa, wafalme kama Daudi, wavuvi kama Petro, wakulima kama Yeremia, Makuhani kama Samueli n.k. hawa wote hawakuishi pamoja. Biblia ni kitabu kitakatifu cha Mungu kwa vile yale yote yaliyotaribiwa kama vile ya kitabu cha Daniel sura mbili na saba yametimia. Machimbo ya akaelojia yanasapoti historia ya kitabu hiki kwa hali ya juu. Zaidi ya yote kitabu hiki kimebadilisha maisha ya watu wengi. Kule Papua New Guinea wakoloni walipoenda waliwacheka wananchi waliokuwa wanasoma Biblia na kuifuata. Wale wananchi wa Papua New Guinea walisema "Mnacheka na wakati ambapo tulikuwa hatuna kitabu hiki, tulikuwa tunakula watu? Nyinyi leo mngekuwa nyama yetu!". Hakuna mtu mwovu aliyebadilika na kusema "Nimesoma Kemia na kubadilika tabia yangu mbaya". Neno la Mungu ni pumzi Yake yenye mafundisho ya kuadilisha ili tuweze kuwa katika mstari Wake.
Kamwe usiseme unalifahamu Neno Lake na hivyo ukaacha kulisoma! Kristo alisaidia manabii kuandika alilijua ndani na nje, Naye aliitwa NENO, bali alilisoma na kulitilia maanani, akisema "Imeandikwa mtu hataishi kwa mkate tu! Bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu". Muhtasari wa Biblia kwa Maneno matatu ni Uumbaji, Maanguko, na Ukarabati.
Hebu tukutane mbinguni kwenye mti wa uzima kwa Neema Yake siku moja, kwa vile tumelithamini Neno Lake ndimo humo upo uzima! Yohana 17:3.

# YALIYOMO


Mwanzo au Uumbaji - Mwanzo 1 na 2 .......... 43
Kuumbwa Mwanadamu .......... 47
Siku ya Saba na ya Mapumziko kwa Binadamu .......... 51
Anguko la Mwanadamu-Jinsi Dhambi Ilivyoingia na Mapambano yalivyoanza hapa Duniani- ..... 54
Shetani Aanguka Toka Mbinguni - Ufunuo 12, Ezekieli 28, Isaya 14, Yohana 3:14-20 na Ayubu 1. .. 58
Adhabu ya Uasi .......... 61
Mtoto wa Kwanza na Kifo cha Kwanza, hakika hasira ni kitu kibaya sana .......... 64
Maisha ya Henoko .......... 68
Nuhu, Safina, na Gharika .......... 72
Mnara wa Babeli .......... 76
Abramu - Baba wa Wenye Imani .......... 79
Kuzaliwa kwa Ishmaeli na Ahadi ya Kuzaliwa kwa Isaka .......... 82
Ibrahimu Azungumza na Mungu na Mvua ya Moto .......... 85
Kuzaliwa kwa Isaka .......... 88
Mtihani Mkubwa kwa Ibrahimu .......... 90
Mke kwa Ajili ya Isaka .......... 93
Ugomvi wa Mapacha na Uzaliwa wa Kwanza .......... 96
Yakobo Achukua Baraka za Esau .......... 98
Familia ya Yakobo .......... 103
Mweleka Wakati wa Usiku .......... 106
Yusufu na Ndugu Zake .......... 109
Yusufu Atoka Jela .......... 113
Wana wa Yakobo Waenda Kununua Nafaka .......... 116
Yakobo Akutana na Yusufu, Na Yusufu alipa mema kwa mabaya .......... 120
Familia ya Yakobo Yaenda Misri .......... 123
Yakobo Amaliza vyema kwa Kutoa Mibaraka kwa Wanawe .......... 126
Kuzaliwa kwa Musa .......... 129
Mateso Yawafanya Wawe Imara na Musa na Kijiti Kilichowaka Moto .......... 133
Musa Awezeshwa kuwa Mbele ya Farao .......... 137
Mapigo ya Misri .......... 140
Pasaka ya Kwanza .......... 143
Kuvuka Bahari ya Shamu .......... 146
Maji Machungu na Mkate wa Mana - Malalamiko yazidi .......... 150
Maji ya Meriba na Kugawanya Uongozi .......... 154
Amri Kumi Katika Mlima wa Sinai (Horebu) .......... 157
Sheria na Hukumu .......... 161
"Wanijengee Patakatifu" .......... 164
Dhambi ya Kuabudu Ndama wa Dhahabu .......... 168
Musa Aenda Tena Mlimani .......... 172
Sababu za Kuwa na Patakatifu .......... 175
Kuwaweka Wakfu Makuhani na Mavazi yao Kwa Uzuri na Utukufu wa Mungu .......... 178
Huduma za Patakatifu .......... 181
Utakatifu wa Huduma za Makuhani: Walitengwa ili wamtumikie Mungu, lakini hawakumtumikia kwa muda mrefu .......... 185
Siku ya Upatanisho .......... 188
Najisi na Visivyo Najisi .......... 191
Mungu na Watu Wake Wanaolalamika .......... 196
Ndugu wa Musa na Uasi .......... 200

Mungu atoa agizo la kutuma Wapelelezi 12 kwenda Kaanani ........ 203
Maji ya Meriba Yamfanya Musa Asiingie Kanaani ........ 208
Safarini na Changamoto Zikiendelea ........ 210
Matoleo na Sikukuu na Kuhesabiwa kwa Waisraeli ........ 214
Kitabu cha Kumbukumbu la Torati - Kisa kinarudiwa mara ya pili wakati Musa anaaga Jeshuruni ........ 217
Wimbo na kifo cha Musa ........ 221
Rahabu na Kamba Nyekundu ........ 225
Kuvuka Mto Yordani ........ 228
Yoshua Akutana na Kamanda wa Majeshi ........ 231
Dhambi ya Akani, Hakuna mtu Ambaye ni Kisiwa........ 234
Yoshua Adanganywa na Wagibeoni na Jua Lasimama ........ 237
Siku za Mwisho za Yoshua ........ 240
Waamuzi - Yoshua 24 na Waamuzi 1 ........ 244
Chagueni Ninyi Leo. ........ 244
Waamuzi wa Kwanza na Uasi wa Israeli ........ 247
- Waamuzi 3-6........ 247
Gideoni- Je, uko Tayari Kuondoa vitu 31,700 Kwenye Maisha Yako ........ 250
Yeftha na Nadhiri ya Kafara ........ 253
Samsoni Mnadhiri wa Mungu Aliyewa na Maguvu Kupita Binadamu yoyote ........ 257
Kitendawili cha Samsoni ........ 260
Mwisho wa Samsoni ........ 263
Hekalu la Sanamu la Mika, uovu wa mtu moja waenea kwenye familia nzima! ........ 266
Uovu Unaowasha Masikio Katika Israeli ........ 269
Naomi Arejea Nyumbani Mkamwana Aliyempenda aenda naye ........ 273
Boazi Amwoa Ruthu ........ 276
Mtoto Samweli, Baraka na Ya Mama Anayeomba na Kumcha Mungu ........ 279
Mtoto Samweli Akiwa Hekaluni ........ 282
Wafilisti Wachukua Sanduku la Agano (Ikabodi) ........ 285
Samweli, Mwamuzi wa Mwisho wa Israeli ........ 289
Sauli Atiwa Mafuta Kuwa Mfalme ........ 293
Sauli Afanya Dhambi kwa Kufanya Huduma ya Kuhani ........ 297
Mungu Ajuta Juu ya Sauli Aliyejali Mapokeo Kuliko Utii ........ 300
Daudi Achaguliwa Kuwa Mfalme ........ 303
Daudi na Goliathi, Vita ni vya Bwana na si Vyetu ........ 306
Urafiki wa Daudi na Yonathani ........ 309
Sauli Aua Makuhani, Baada ya Daudi kuzungumza nao ........ 313
Abiathari Akimbilia kwa Daudi ........ 317
Daudi, Nabali na Abigaili ........ 320
Sauli Amwinda Tena Daudi ........ 323
Mchawi wa Endori ........ 327
Madanganyo ya Shetani ........ 331
Kifo cha Sauli ........ 334
Daudi Atawala Hebroni na Israeli Yote ........ 338
Sanduku la BWANA Larudi ........ 341
Kurudisha Hisani Kupitia kwa Mefiboshethi ........ 344
Dhambi Kubwa ya Daudi ........ 347
Adhabu ya Daudi ........ 350
Toba ya Daudi ........ 353
Uovu Nyumbani mwa Daudi ........ 356

Absalomu na Yoabu ..... 359
Matamanio Yasiyo Matakatifu na Yenye Ubinafsi ..... 362
Absalomu Afanya Vita na Babaye ..... 365
Absalomu Auawa ..... 368
Daudi Arejea Katika Ufalme ..... 371
Mashujaa wa Daudi ..... 374
Daudi Awahesabu Israeli ..... 376
Kutawazwa kwa Sulemani ..... 379
Zaburi - Nyimbo na Ibada ..... 382
Sulemani na Maagizo ya Baba Yake ..... 386
BWANA Amtokea Sulemani ..... 389
Maneno ya Hekima ..... 392
Mithali na Mhubiri..... 396
Mhubiri au Kohelethi..... 399
Kujenga Hekalu ..... 402
Ujenzi wa Hekalu Wakamilika ..... 405
Hekalu Lawekwa Wakfu ..... 407
Jibu la BWANA kwa Sulemani ..... 411
Wimbo Ulio Bora au Wimbo wa Sulemani ..... 414
Sulemani Amwacha Mungu ..... 418
Rehoboamu Mwana wa Sulemani Arithi Yuda, Jinsi ya sisi Kuepuka Majuto ..... 421
Ufalme wa Israeli Wagawanyika ..... 423
Mkono wa Yeroboamu Wapooza ..... 425
Wafalme wa Yuda na Israeli ..... 427
Wafalme na Nabii Eliya-Mtishbi ..... 431
Mwana wa Mjane wa Sarepta Afufuliwa ..... 434
Manabii wa Baali na Ashera Mlimani Karmeli ..... 437
Eliya Apungukiwa Ujasiri na Kukimbia ..... 440
Eliya Amtia Mafuta Mrithi Wake ..... 443
Shamba la Nabothi ..... 446
Siku za Mwisho za Ahabu ..... 449
Yehoshafati, Ahazia na Eliya ..... 452
Nabii Eliya Atwaliwa Mbinguni - Ni Baraka Gani Ungeomba Wewe Ungeulizwa ..... 454
Watoto Wakorofi Waadhibiwa ..... 457
Mwanamke Mjane na Mafuta na Mwanamke Mshunemu ..... 460
Chakula Chenye Sumu na Shoka Lililozama ..... 463
Jemedari Naamani na Mjakazi Mtumwa ..... 466
Ukoma wa Naamani Wahamia kwa Gehazi ..... 469
Magari ya Moto ..... 471
BWANA Awapigania Israeli ..... 473
Hazaeli Awa Mfalme wa Shamu ..... 476
Utawala wa Yehu ..... 479
Yoashi-Mfalme Mtoto ..... 482
Kwaya Iliyoshinda Vita ..... 486
Miaka ya Uovu wa Wafalme ..... 489
Wafalme Zaidi ..... 493
Makabila 10 ya Israeli Yalivyopotea ..... 497
Mfalme Hezekia Afanya Israeli Imrudie Mungu kwa Matengenezo na Uamsho ..... 499
Kuugua kwa Hezekia na Jua kusimama ..... 503
Mfalme Manase na Yosia ..... 507

Yosia Afanya Matengenezo ........ 510
Ufalme wa Mwisho wa Yuda ........ 515
Ezra – Kuhani aliuelekeza moyo wake kuitafuta sheria ya Bwana na kuitenda! ........ 520
Ezra na Nehemia wana Uamsho na Matengenezo ........ 523
Nehemia – Rafiki ya Mfalme Asema MUNGU Wetu Atatupigania ........ 526
Nabii Isaya - Mwaliko wa Njooni tusemezane ........ 530
Ujumbe Zaidi wa Isaya ........ 533
Ujumbe wa Yeremia Nabii - Baruku Mwandishi - 625 KK ........ 535
Ujumbe Zaidi wa Yeremia ........ 539
Nabii Ezekieli ........ 541
Ujumbe wa Ezekieli Unaendelea ........ 545
Esta Awa Malkia ........ 547
Esta na Wayahudi Wafanya Maombi Maalumu ........ 550
Mordekai Apandishwa Cheo na Wayahudi Wajitetea ........ 553
Mtu wa Mungu Ayubu ........ 556
Danieli Aenda Uhamishoni ........ 562
Somo la Chakula ........ 564
Mfalme Aota Ndoto ........ 567
Falme Zitakazotawala Dunia ........ 570
Umuhimu wa Unabii wa Danieli 2 ........ 572
Kurudia unabii wa Danieli 2 kwa undani zaidi ........ 576
Kulazimishwa Kusujudu Sanamu ........ 579
Mfalme Nebukadneza Aishi Porini ........ 583
Kiganja cha Mkono Kisicho na Damu Chaandika Ukutani ........ 587
Danieli Atupwa Kwenye Pango la Simba ........ 591
Wanyama wa Ajabu ........ 594
Tafsiri ya Ndoto ya Danieli 7 ........ 596
Maono ya Kondoo Mume na Beberu ........ 599
Danieli Azidi Kufunuliwa Siri za Unabii ........ 602
Unabii wa Siku 2300 Wafunuliwa ........ 604
Maarifa Kuongezeka ........ 607
Upendo wa Mungu kwa Watu Wake ........ 611
Ujumbe wa Yoel-Nitakuachaje, Nitakuokoaje, Eh Israeli? ........ 615
Nabii Amosi ........ 618
Ujumbe wa Mika ........ 620
Yona - Nabii Aliyemezwa na Samaki ........ 623
Yona Ndani ya Samaki ........ 625
Kujenga Hekalu ........ 628
Ujumbe wa Nabii Nahumu ........ 631
Obadia siku ya BWANA ........ 634
Habakuki – Anamwuliza Mungu Maswali ili apate Tumaini, akiona Kimya anamwuliza “Hutafunga goli tena?” ........ 636
Ujumbe wa Sefania ........ 639
Zekaria-Ujumbe kwa Waliorejea Toka Uhamishoni ........ 641
Malaki – Ujumbe wa Matengenezo, Bwana Atafungua Madirisha na si Milango! ........ 644
Je, Mungu ametusahau? Watu walijiuliza ........ 648
Vitabu vinne vya injili. ........ 652
YESU Alikuwako siku zote, na anaendelea kuishi milele. ........ 656
Unabii wa kuzaliwa kwa Yesu Masihi na BWANA wetu. ........ 659
Kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji msafisha njia wa Masihi. ........ 662

Kuzaliwa kwa Yesu Masihi na Mwana wa Mungu. .......... 665
Mamajusi kutoka mashariki wamtembelea Yesu.......... 669
Mathayo 2. .......... 669
Yesu abarikiwa hekaluni akiwa na siku 40. .......... 673
Yesu hekaluni akiwa na miaka 12. .......... 677
Utoto wa Yesu na Yohana mbatizaji. .......... 681
Yesu Asimikwa kwa Ubatizo mto Yordani. .......... 684
Yesu anajaribiwa na Shetani nyikani. .......... 687
Kuita wanafunzi wa kwanza .......... 691
Kuita wanafunzi wa kwanza .......... 694
Yesu anafanya muujiza wa kwanza kwenye arusi Kana. .......... 699
Yesu apindua meza za hekalu, na kutakasa hekalu. .......... 702
Nikodemu mwanafunzi wa Yesu aliyekuja usiku. .......... 705
Mwanamke Msamaria wa Sikari kisimani. .......... 710
Yohana awekwa kizimbani na kuuwawa. .......... 714
Yesu ananza kazi kwao Nazareti alipolelewa .......... 718
Yesu akataliwa kwao Nazareti. .......... 721
Wavuvi waitwa tena kuwa wanafunzi. .......... 725
Mathayo aitwa awe mwanafunzi, na afanya karamu ya kuaga wenzake. .......... 728
Mambo ya kufanya siku ya Sabato. .......... 732
Kuponya siku ya Sabato. .......... 735
Mlango wa kuingia mbinguni ni Mwembamba. .......... 738
Mlima wa baraka-Heri, chumvi, taa. .......... 741
Mlima wa baraka-Sheria na kuishi maisha ya ukristo. .......... 745
Wana Heri au Wana furaha, au Wamebarikiwa. .......... 750
Sala ya BWANA aliyotufundisha tuombe. .......... 753
Ombeni nanyi mtapewa, Bisheni nanyi mtafunguliwa, tafuteni nanyi mtapata. .......... 757
Mtumishi wa akida wa Kirumi aponywa. .......... 761
Mariamu Magdalena na Marhamu ya upendo. .......... 764
Marita na Mariamu dada wawili waliomshughulikia Yesu. .......... 769
Mpanzi au mpandaji mbegu, Yesu afundisha kwa mifano. .......... 772
Mifano ya Yesu. Upepo wamtii. .......... 777
Mitume 12 waenda kazini. .......... 780
Kutuma wanafunzi 70 umishonari. .......... 784
Msamaria mwema mwenye huruma. .......... 787
Mungu anatuhimiza tuutafute ufalme Wake na haki Yake kwanza. .......... 790
Gharama ya kuwa mwanafunzi wa Yesu. .......... 793
Ufalme wa mbinguni ni Lulu ya thamani, au nyavu ya samaki. .......... 796
Mikate mitano, samaki wawili kulisha maelfu. .......... 799
Petro atembea juu ya maji. .......... 803
Wanafunzi wanarudi nyuma na wengine watoroka. .......... 806
Mwanamke aliyefumaniwa akizini. .......... 808
Kipofu aponywa. .......... 812
Kipofu aliyefumbuliwa macho atengwa ushirika. .......... 815
Mwenye pepo Gerasi. .......... 818
Yesu amponya binti Yairo, na mama aliyeugua miaka 12. .......... 821
Huwezi kutumikia mabwana wawili. .......... 824
Mfano wa tajiri na Lazaro. .......... 826
Kurudisha shukrani. .......... 828
Dhambi yaweza kumfuata mtu kanisani. .......... 831

Zakayo mtu mfupi apanda mti. .................................................... 834
Imani ya mwanamke mkakanayo. .................................................... 838
Kulishwa kwa watu 4000 mikate na samaki mara ya pili. .................................................... 842
Kubeba msalaba na kukana nafsi. .................................................... 846
Wanafunzi washindwa kutoa pepo. .................................................... 849
Ni nani mkubwa katika ufalme wa Mungu. .................................................... 852
Je, ni halali kumpa mke talaka au kuachana? .................................................... 856
Waacheni watoto wadogo waje Kwangu. .................................................... 860
Kijana tajiri na mtawala. .................................................... 865
Waajiriwa asubuhi na wale wa jioni, walipwa sawa sawa. .................................................... 869
Kukaa mkono wa kuume au kushoto mbinguni. .................................................... 871
Kipofu Batimayo. .................................................... 874
Kulipa kodi ni halali. .................................................... 877
Twapasa kusamehe watu kama Mungu anavyotusamehe. .................................................... 880
Hosana mbarikwa ajaye kwa Jina la BWANA. .................................................... 884
Mtini kukauka. .................................................... 888
Mkulima mwenye shamba na watenda kazi waovu. .................................................... 891
Masadukayo, ndoa na ufufuo.................................................... 893
Ipi ni amri kubwa kupita zingine. .................................................... 896
Ole wa Mafarisayo. .................................................... 899
Mafarisayo. .................................................... 902
Yesu anarudi upesi, Je dalili za kuja Kwake ni zipi? .................................................... 905
Dalili za siku za mwisho. .................................................... 908
Wanawali watano wajinga, na watano werevu. .................................................... 913
Kutumia talanta zetu ili ziwe na faida. .................................................... 915
Pasipoti ya kusafiria Mbinguni. .................................................... 918
Yesu anamfufua Lazaro. .................................................... 922
Wanapanga kumwua Yesu .................................................... 926
Wayunani wanamtafuta Yesu. .................................................... 929
Kualikwa arusini. .................................................... 932
Mwanakondoo aliyepotea, sarafu iliyopotea. .................................................... 935
Mwana mpotevu au mtoto aliyekimbia kwao. .................................................... 938
BWANA aosha miguu. .................................................... 942
Pasaka ya mwisho. .................................................... 946
Msifadhaikeni mioyoni mwenu. .................................................... 950
Yesu mzabibu wa Kweli. .................................................... 954
Sala ya Yesu kwetu wote. .................................................... 957
Yesu anakamatwa. .................................................... 961
Yesu kwa Pilato. .................................................... 965
Taji ya miiba. .................................................... 969
Yesu anakata roho. .................................................... 975
Mazishi ya Yesu. .................................................... 980
Kufufuka kwa YESU: Habari Njema Kupita Zote Ulimwenguni! .................................................... 985
Njia ya Emmaus: Kleopa na Mwenzake wapata masomo ya Biblia! .................................................... 989
Simoni na Yohana wanaenda kaburini kuhakikisha. .................................................... 993
Yesu awatokea wanafunzi Wake kwa siku 40. .................................................... 996
Yesu amwimarisha Petro. .................................................... 999
Yesu Anapaa juu mbinguni. .................................................... 1002
Je, Yesu anafanya nini mbinguni sasa? "Tuna Rafiki mbinguni." .................................................... 1007
Kusimulia Kisa cha Wokovu kwa dakika tatu!-Wokovu ni nini?.................................................... 1011

Kungoja Roho Mtakatifu/Pentekoste Yerusalemu. ........ 1014
Pentekoste. ........ 1017
Petro anahubiri. ........ 1021
Kiwete aruka ruka. ........ 1024
Mitume wanaingia Gerezani kwa mara ya kwanza........ 1027
Anania na Safira. ........ 1031
Mitume wawekwa gerezani mara mbili. ........ 1034
Stefano auwawa. ........ 1037
Sauli atesa watakatifu na kanisa. ........ 1041
Filipo na towashi wa Ethiopia (Kushi). ........ 1043
Sauli atokewa na Yesu. ........ 1046
Tabitha au Dorkasi mama mkarimu afufuliwa. ........ 1049
Kornelio wa mataifa Maombi yake yalisikiwa. ........ 1051
Hakika Mungu hana upendeleo. ........ 1054
Petro atolewa na Malaika gerezani. ........ 1057
Wayahudi wakataa injili, Ukristo waenda kwa mataifa. ........ 1061
Paulo apigwa mawe Lystra. ........ 1064
Baraza la Mitume laandika barua ihusuyo wamataifa wanaomwamini Yesu. ........ 1067
Paulo na Sila waimba gerezani. ........ 1072
Watu waliopindua ulimwengu juu chini. ........ 1076
Akila, Prisila, na Apolo. ........ 1080
Vitabu vya uovu vyachomwa moto. ........ 1083
Efeso na mungu wao wa kike aitwaye Artemi. ........ 1085
Paulo awaaga waumini. ........ 1088
Paulo akamatwa. ........ 1091
Paulo ajitetea na kurudia Historia ya injili. ........ 1094
Masadukayo na Mafarisayo wamgombania Paulo. ........ 1096
Paulo aenda Kaisaria na Jeshi. ........ 1099
Paulo mbele ya Gavana Feliki. ........ 1101
Paulo anakata rufani kwenda Rumi mbele ya Agripa. ........ 1104
Paulo ashuhudia kisa chake tena. ........ 1107
Paulo amkatisha shauri Herode Agripa. ........ 1109
Kuvunjikiwa merikebu na kuogelea. ........ 1112
Kisiwani malta na ukarimu wao. ........ 1115
Paulo ashuhudia Rumi na kuandika barua kwa makanisa. ........ 1118
Barua za Paulo, Mitume na Yuda na Yakobo. ........ 1121
Warumi. Tunaokolewa kwa Imani, kupitia Yesu tu! Si kwa matendo ya sheria. ........ 1124
Nami siionei haya injili! ........ 1124
Shida za waumini wapya zajadiliwa. ........ 1128
Tunapokuwa wanyonge ndiyo tuna nguvu. ........ 1132
Tunda la Roho dhidi ya matendo ya mwili. ........ 1136
Mahusiano ya wazazi, watoto, wake, waume, mabwana na watumwa. ........ 1139
Furahini katika BWANA tena nasema furahini ........ 1143
Kama tulivyompokea Kristo tuenende vivyo hivyo katika Yeye. ........ 1146
Tuombe bila kukoma ........ 1149
Asiyefanya kazi na asile. ........ 1152
Tabia ya Mchungaji na Shemasi ........ 1155
Nimevipiga vita vizuri, Mwendo nimeumaliza, Taji inaningojea. ........ 1158
Tabia ya Mchungaji, tabia ya mzee wa kanisa. ........ 1161
Msamehe Onesimo na mchukue kama Ndugu ........ 1164

Yesu ni bora kupita vyote. Kafara Yake, ni bora, Ukuhani Wake ni Bora………. ........................... 1168
Imani bila matendo ya kumpendeza Mungu, imekufa........................................................................ 1172
Tazameni pendo la ajabu! Mungu ni Upendo. ................................................................................... 1182
Naomba ufanikiwe katika mambo yote.............................................................................................. 1188
MUNGU anaweza kutulinda tusijikwae, tukimruhusu. .................................................................... 1192
UFUNUO. Upande wa Mungu unashinda, Haleluya! Mungu atahukumu na kuwazawadia watakatifu. Heri ya Asomaye. ............................................................................................................ 1195
Makanisa saba ya Asia Ndogo. ......................................................................................................... 1199
Ni nani awezaye kukifungua kitabu? ................................................................................................ 1202
Shetani alivyoanguka na malaika zake wakaja duniani. ................................................................... 1205
Mnyama wa kwanza na wa Pili. ........................................................................................................ 1209
Malaika wanne na watakatifu 144,000. ............................................................................................ 1212
Kuepuka mafundisho ya uongo. ........................................................................................................ 1215
Jehanamu I......................................................................................................................................... 1218
Jehanamu II ....................................................................................................................................... 1223
Tazama maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu. ...................................................................... 1226
Mbinguni milele na milele. ............................................................................................................... 1229
Yerusalemu mpya yashuka chini, kila goti litapigwa kwa Mwenyezi MUNGU na Kila ulimi utakiri. ......................................................................................................................................... 1234
ELIMU Ya Kikristo ndiyo Elimu ya milele na bora kupita zote......................................................... 1238
KUFANYA MARAFIKI WA MUNGU ................................................................................................ 1243
Jinsi Mungu Anavyompenda Mwanadamu ........................................................................................ 1246
Pambano kuu limekwisha! Vidogo na vikubwa, hai na visivyo hai vyasema Mungu ni Upendo! .. 1251
Jinsi ya kukuza Ubongo wako ili uwe na Akili sana (genius) Kwa kutafakari yale ya Mbinguni na kuyafanyia kazi, hatua kwa hatua ...................................................................................................... 1254
Hatua za ufanisi katika maisha yako.................................................................................................. 1257

# AGANO
# LA
# KALE



**SIKU YA 1**
**(January 1)**

# Mwanzo au Uumbaji - Mwanzo 1 na 2

**(Mwanzo-Mwandishi Musa miaka ya 1500KK).**



Je, umeshawahi kujiuliza kwamba vitu vyote duniani vilitoka wapi? Au wazazi wako walitoka wapi? Labda ulijibu kuwa wametoka kwa babu na bibi. Na babu na bibi walitoka wapi? Na mwishowe wale mababu wa mwanzo walitoka wapi? Au kwamba nini kilikuja kabla ya kingine. Kwa mfano, Je, ni kuku au ni yai? Pengine umesikia kwamba mimea ilitoka kwenye mbegu, na mbegu kwenye maua. Mzunguko unaendelea hivyo hivyo. Na Milima je? Mito, bahari na vilindi. Je, vilikuwa hivyo hivyo wakati wote, au vilikuwa na mwanzo? Kuanzia shule za msingi, tunasoma sayansi na kustaajabu jinsi jicho, ubongo, mguu, kompyuta vinavyofanya kazi. Hivi havijatokea tu vyenyewe kwa bahati, kuna injinia aliyevibuni na kuvianzisha.

Ulimwengu wetu ni wa zamani sana. Tukihesabu kutokana na miaka ya watu katika Neno la Mungu, inakadiriwa kuwa na miaka 6000 hivi. Hakuna anayejua kwa uhakika siku na saa au tarehe ya ulimwengu wetu kuumbwa. Hata hivyo, jambo muhimu ni kuwa Mungu aliumba ulimwengu, jua, mwezi, na vyote vilivyomo. Mungu alikuwepo. Mungu amekuwepo wakati wote. Yeye hana mwanzo wala mwisho kama vile tulivyo binadamu. Hili ni jambo ambalo ni vigumu kueleweka

kwa akili za kibinadamu. Lakini Mungu ni mkuu kuliko sheria za Sayansi kama vile muda, mahali au maada maana Ndiye aliyeviumba. Neno la Mungu linaumba. Akisema tu mambo yanakuwa Papo hapo! Haichukui nukta! Yeye Alikuwepo, Yupo na ataendelea kuwapo. Kwa fikira ya binadamu aliye na mwanzo na mwisho ni vigumu kuelewa. Bali Mungu ni wa milele, wa Kwanza na wa Mwisho, Alfa na Omega.

Neno la Mungu linaeleza bila mashaka kuwa, "Hapo Mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi". Mwanzo 1:1. Ni dhana inayoeleweka. Mababu na mababu walielewa hili. Hata kama waliabudu vitu vingine, walijua kuwa wameumbwa na Mwenyezi Mungu. Sura ya kwanza ya Biblia inafanana na ile ya Yohana moja isemayo, "Hapo Mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu … wala pasipo Huyo hakikufanyika chochote kilichofanyika."

Tunaambiwa kuwa "Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa tena utupu, na giza nene lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji. Pengine maji yalisikika yakibubujika. Roho wa Mungu alitulia kwenye maji, Mungu akaamuru "na iwe nuru". Mungu akaiona nuru kuwa ni njema. Mungu akatenga Nuru na giza. Mungu akaiita nuru mchana na giza akaliita usiku. Ikawa jioni, ikawa asubuhi", siku moja ikawa imemalizika. Bwana aliumba siku kwanza jioni, asubuhi kisha jioni tena, saa 24! Hivyo siku Mungu aliziumba zianze jioni na kuisha jioni. Wakati Warumi walipoitawala dunia, walibadilisha na kufanya siku ihesabiwe kuanzia saa sita ya usiku na kuisha saa sita ya usiku.

Katika Kitabu cha Mwanzo, siku ya kwanza ya juma, haikusemwa ni siku gani. Lakini katika vitabu vya Injili tunaambiwa kuwa Yesu alifufuka siku ya kwanza ya juma. Hivyo, nuru iliumbwa siku ya kwanza ya juma ambayo ni Jumapili kwa siku zetu za Kiswahili. Mungu aliumba kwa Neno Lake, vitu vikatokea. Hakuchukua muda kama sisi kutengeneza kitu fulani, au kuchukua maada ya mtu mwingine au vitu vya mtu mwingine ili kuumba! Sisi tukitaka kutengeneza kiti, tunahitaji misumari na mbao. Yeye ana uwezo wote, nguvu na maarifa yote. Kwa kutamka tu, mambo yalifanyika, ndivyo ilivyokuwa katika uumbaji. Aliumba pasipo kutumia kitu cho chote. Inasemekana mtu fulani aliwahi kusema kuwa anaweza kuumba. Akasema, nitachukua udongo nianze kuumba mwanadamu, akaambiwa hapana, udongo ni wa Mungu, anza na mali ghafi zako!

Kwa kutamka tu giza likatoweka, kukawa na mwanga, ila hakukuwa na anga mpaka siku ya pili. Mungu aliendelea kuumba, akiwa na mipango mikubwa ya kumfanyia makazi mwanadamu anayempenda. Mungu akasema "na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji".

Mungu akalifanya anga, akayatenga maji yaliyo juu ya anga na yale yaliyo chini ya anga. Mungu akaliita anga mbingu. Siku ya tatu Mungu akatenga maji na nchi kavu, "maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, ili pakavu paonekane, akapaita pakavu nchi, na makusanyiko ya maji bahari. Mungu akasema nchi na itoe majani, mche utoao mbegu na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi zake. Ikawa hivyo, Mungu akaona kuwa ni vyema." Anga ndiyo lina hewa ambayo viumbe vyote, mimea na wanyama wanavuta.

Siku ya nne Mungu akaumba mianga mikubwa miwili, yaani, jua na mwezi, akaumba na nyota pia. Akasema “na iwe mianga katika anga la mbingu itenge kati ya mchana na usiku, nayo iwe ndiyo dalili na majira na siku na miaka”. Mianga hiyo ikawa ya kutia nuru juu ya nchi. Mwanga mkubwa ‘jua’ ukawa wa mchana na mwanga mdogo wa mwezi ukawa wa usiku. Jua liko umbali wa kilometa milioni 150 toka duniani, lakini inachukua dakika nane kwa mwali wa jua kutufikia. Hewa ya Haidrojeni ndiyo inayosaidia jua kama vile moto unavyotengenezwa. Jua ni kubwa kwa dunia mara milioni 1.3. Aliumba mwezi kuzunguka dunia kwa siku 28, na dunia kuzunguka jua kwa siku 365. Wataalamu wengi sasa wanagundua kuwa baadhi ya zile tunazoiita nyota, ni sayari ziingine ambazo idadi yake ni mabilioni. Watu waliojaribu kuhesabu nyota kwa macho ya kawaida, kukiwa shwari angani wamefikia nyota 5000 tu! Kweli Mungu wetu ni wa Ajabu. Mungu hakuwa na haraka, angeweza kuumba vyote hivi kwa sekunde moja, lakini hakufanya hivyo. Dunia ikaanza kuonesha uzuri wa ajabu, jua likitua na rangi ya chungwa kuonekana, na nyota kuonekana usiku. Mungu alikuwa anaumba ulimwengu uwe wa kudumu milele. Aliuumba kwa uzuri wa ajabu.

Siku ya tano ilipoanza kulikuwa na sauti ya miti ikiyumba bali hakukuwa na sauti ya paka au tembo akilia! Mungu akasema, “Maji yajawe kwa wingi na kitu kiendacho chenye uhai, na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu. Mungu akaumba nyangumi wakubwa na kila chenye uhai kiendacho majini. Maji yalijawa navyo kwa wingi.” Akaumba kila ndege arukaye, hawa wakaimba na kumsifu Muumba wao.

Siku ya sita ilipofika, Mungu akasema, “Nchi na izae kiumbe hai kwa jinsi zake, mnyama wa kufugwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake, ikawa hivyo”. Siku ya tano na ya sita zilikuwa ni siku za ajabu wakati mamilioni ya wanyama mbali mbali kwa maumbo na rangi mbalimbali walipotokea. Nimepata kutembelea shamba la samaki na kuona samaki wa kupendeza macho, wala sikutaka kutoka mahali pale. Pengine umeona rangi za ndege na vipepeo, na hata wale wanyama wakubwa ambao watu wanakuja kutoka kila mahali duniani ili waweze kuwaona. Kuanzia na wale wanaoitwa ‘big Five’ au wakubwa wanne, nao ni Tembo, Simba, Twiga na Kifaru!

Tembo, simba, twiga, faru, nyati, fisi, kiboko, mamba, na wengine, waliumbwa siku ya sita. Kuna wengine wadogo sana kama panya na wengine wakubwa sana. Wadudu tu ni mamilioni wa aina tofauti bila ya kuzungumzia wanyama wengine! Ndege wakaanza kuimba na kumsifu Mungu wao, wakiruka hapa na pale. Sokwe wakatokea na kurukaruka mitini wakifurahi. Kweli Mungu wetu ni wa ajabu. Bila shaka wanyama waliangaliana na kushangaa jinsi maumbile yao yalivyo tofauti. Pengine twiga aliangalia na alipomwona kobe, naye aliwaza, “hivi ni mnyama gani huyu, anayetembea pole pole hivi?” Wanyama waliishi pamoja bila kuogopana, ilikuwa ni jumuiya moja. Hakuna aliyemwinda au kumla mwingine Wengine wenye masikio makubwa na wengine wenye pua kubwa au mikonga, na wengine pembe za kati kama kifaru. Mungu alifurahi kuona hawa wanyama na akaona kwamba kila kitu ni chema.
Piga picha ya msafara wa wanyama wakitembea kwenda mahali fulani. Tunaweza



kuchora wanyama kwenye karatasi ila hatuwezi kuumba. Ni Mungu Peke Yake Aliye na uwezo wa kuumba, na ndiyo maana kila kiumbe kina thamani kubwa. Usimpige paka, mbwa, punda au ng'ombe bila sababu kwa kuwa ni viumbe wa Mungu! Hata kuharibu mimea au miti bila sababu si jambo zuri. Ni uwakili mzuri kutunza vitu tulivyopewa na Bwana. Nuia kusoma Neno la Mungu kila siku, Nalo litakusaidia kuwa na tabia njema, na pia kujibu maswali yote uliyo nayo moyoni, hivyo utakuwa wakili mwema. Ni vigumu kueleza kwa maneno ya binadamu uzuri wa uumbaji, mionjo, sauti, harufu, hisia n.k

Yote unayojifunza kutoka kwa wazazi, walimu, na kujisomea yanasaidia kukufanya uwe mtu bora. Kusudia leo kujisomea Neno la Mungu kila siku.

*Katika ibada ya familia hebu waachie watoto washiriki sehemu. Acha wote walete Bibilia zao na kila mmoja asome mstari mmoja au miwili. Kisha wimbo au tenzi fulani inayojulikana iimbwe, ikifuatiwa na maombi. Kwa hili, Kristo ametoa mfano. Sala ya Bwana haikukusudiwa kurudiwa tu kama mfumo au desturi fulani, lakini ni kielelezo cha jinsi maombi yetu yanavyopaswa kuwa-sahili au rahisi, ya bidii, na ya kina. Katika ombi rahisi mwambie Bwana mahitaji yako na onyesha shukrani kwa rehema Zake. Kwa hivyo unamwalika Yesu kama mgeni aliyekaribishwa ndani ya nyumba na moyo wako. Katika familia maombi marefu kuhusu vitu vya mbali hayapaswi kuwepo. Vinafanya saa ya maombi kuwa ya kuchosha, wakati inapaswa kuzingatiwa kama fursa na baraka. Fanya msimu uwe wa kupendeza na wa kufurahisha.

---

Ni nini kilikuwapo kabla ya Mungu kuumba dunia, jua au nyota? Je, nini kiliumbwa siku ya tatu? Mungu aliumba nini siku ya Tano? Je, vile vitu ambavyo Mungu aliviumba siku ya kwanza mpaka ya sita bado vipo hata leo? Viorodheshe vile unavyoviona kwa siku zake za kuumbwa. Unajifunza somo gani hapa?

**SIKU YA 2**
**(January 2)**

# Kuumbwa Mwanadamu

**Mwanzo 1 na 2**



Kabla siku ya sita haijamalizika, Bwana aliumba mtu kwa mfano Wake, kwa mfano Wake Mungu alimwumba mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mungu akasema "Na tufanye mtu kwa mfano Wetu, wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani … na kila kiumbe" Mwanzo 1:27. Mungu akawaambia, "Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha, mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi." Hii ilikuwa amri ya kwanza kuandikwa kwenye Biblia! Mungu akampa binadamu kila mche utoao mbegu ulio juu ya uso wa nchi yote pia na kila mti ambao matunda yake yana mbegu viwe ndiyo chakula chake. Binadamu alipewa ale vyakula ambavyo vinatokana na mimea tu. Baada ya gharika ndipo hali ikabadilika. Wanyama wote walikuwa wana urafiki, hakuna aliyemwinda, kumnasa au kumvizia mwingine. Katika mbingu mpya na nchi mpya, hali itarudi kama ile ya awali. Hakuna kitakachokufa! Kwa maneno mengine, watu wote watarudia lishe ya Mwanzo 1:29. Hakuna kiumbe kitakachoua kingine na kula. Tutakuwa na vyakula vizuri ajabu!

Kuanzia leo, panga mkakati wa kuwa mbinguni!Nami napanga! Adamu alipewa kazi ya kufanya, hata kabla ya kupewa mke, kazi ni muhimu sana!

Baada ya Mungu kuumba vitu vyote, ndipo akamuumba binadamu. Siku tano za kwanza Mungu alikuwa anamtengenezea binadamu zawadi, yaani, riziki na vitu vya kumfurahisha moyo pia. Mungu alitayarisha riziki zetu hata kabla ya kutuumba. Zawadi ya vito vya thamani kama dhahabu, shaba, chuma. Zawadi ya chakula, zawadi ya wanyama wa kuvutia macho alipokuwa akitalii katika bustani ya Edeni. Mungu alimpatia binadamu zawadi za ajabu. Watu wengine wanafikiri kwamba Mungu hapendi mapambo ya vito! La hasha, Mungu Ndiye muumbaji wa uzuri na mazuri yote! Shida ni sisi binadamu kutumia vitu tulivyopatiwa kwa lengo la kujionesha au kiburi kwa kuzibandika kama maonyesho kwa utukufu wetu, ili watu watuone nazo badala ya kumtukuza Mwumbaji. Zamani kulikuwa hakuna haja ya mtu kuzunguka hapa na pale kuepuka uzio, kwani binadamu hakuwa na haja ya kuweka uzio, au miiba ili mtu asipite kwake. Hakukuwa na haja ya kuwa na nyumba. Bustani ya Edeni ilikuwa na uzuri uliopita kifani kuelezea, na hakukuwa na madhara. Edeni ina maana furaha (pleasure) Mvua haikuwapo kwa kuwa umande uliipatia mimea maji ya kutosha. Hapakuwa na haja ya vitanda, kwani mandhari ambayo Mungu alimwekea binadamu ilipita uzuri wa vitu vyote ambavyo binadamu anaweza kuvitengeneza. Binadamu alilala bustanini katikati ya maua yenye kupendeza. Akitaka kula alichuma matunda na kuweka kwenye majani kama sahani akala, hakuwa na haja ya kuosha sahani na sabuni baada ya hapo kwani vijidudu au virusi havikuwepo. Pengine hata chakula chote kiliyeyuka na kuwa lishe mwilini. Pengine Mungu aliwaza na kusema, “Bila shaka binadamu atafurahia makazi haya niliyoandaa ili kumpatia furaha. Bila shaka atanipenda kama ninavyompenda, na tutakuwa na mahusiano na mazungumzo matamu “.

Katika kuumba, Mungu aliumba viumbe vingine vyote kwa kutamka. Alipotamka, vitu vikatokea. Lakini alipomuumba mwanadamu, Biblia inasema alichukua udongo akamfinyanga mwanadamu. Aliumba kichwa, uso, mwili. Alimwumba binadamu aliyekuwa na uwezo wa kuona, kusikia, kuonja, kuhisi na kunusa. Mwenye utashi wa hali ya juu kupita viumbe vyote. Kisha “Mungu akampulizia puani, pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai. Bila pumzi ya uhai, ulikuwa ni mwili tu bila uzima, bali baada ya Mungu kumpulizia pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai. Kwa mahesabu basi, binadamu ni udongo, kujumlisha na Pumzi ya Mungu ya uhai. Binadamu amefanya mengi, lakini hawezi kuumba. Ni Mungu Peke Yake aliye Mwumbaji. Aliweka mti wa uzima katikati ya bustani ya Edeni na mti wa ujuzi wa kujua mema na mabaya. Akaweka mito minne ambayo iliinywesha bustani, nayo iliitwa Pishoni, Gihoni, Hidekeli (Tigris) na Frati. Mungu akampatia Adamu na Hawa kazi ya kuilima bustani na kuitunza. Akamwambia “Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika”.

Mungu alimwumba Adamu kwanza, lakini hakuona wa kuweza kumsaida aliyefanana Naye. Hii ilimpa Adamu ukiwa, na ilimfanya amthamini Hawa alipokuwa ameumbwa. Bila shaka viumbe vyote vilikuwa rafiki. Alipowaita pengine waliitikia wakasimama, bali hawakuweza kuzungumza. Pengine walitikisa mkia au kuruka.

Ndipo Mungu akasema “si vema huyo mtu awe peke yake, Nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye”. Mungu akamletea Adamu wanyama ili awaone na kuwapa majina. Adamu akawapa majina kila mnyama wa kufugwa. Adamu akajisikia anapata usingizi mzito. Mikono ile yenye uwezo wote, ikagusa, na kutoa ubavu mmoja wa Adamu, na kurudisha kila kitu sawa bila kidonda. Adamu alipoamka alimwona kiumbe mwingine aliyefanana naye akasema, “huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu. Basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume. Kwa sababu hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja”. Basi kile ambacho Mungu amekiweka pamoja mwanadamu asikitenganishe. Adamu na Hawa walipatiwa vazi la pekee sana, walikuwa wamevikwa utukufu wa Mungu. Picha zetu za kibinadamu, haziwezi kuonesha hali halisi kwani watu wamewachora bila nguo, na hili si jambo la Kweli! Ila ni nani awezaye kuchora vazi la utukufu wa Mungu? Mungu alimwumba Hawa kuwa msaidizi, hakuchukua kipande cha kichwa, kuonesha kwamba amtawale mume wake, au kipande cha mguu ili awe mtumwa wa mume wake.

Kwa mujibu wa Maandiko, mume ndiye aliyepewa utawala wa nyumba, na mke ni msaidizi. Mungu aliumba mwanamume mmoja na mwanamke mmoja – Adamu na Hawa na siyo Adamu, Hawa na Neema yaani mitara! Siyo Adamu na Yusufu, yaani ushoga Hii ikionesha kuwa si mpango wa Mungu kwamba mume awe na mwenzi zaidi ya mmoja au kuwa na ndoa za jinsia moja. Aliwapatia mbaraka wa ndoa akionesha kuwa ndoa ni kati ya mume na mke na si mwanamke na mwanamke au mwanamume na mwanamume. Mume na mke ndio wanakamilisha mfano wa Mungu. Hawa ndio wangeweza kutimiza Agizo la kwanza ambalo lilisema, “zaeni”. Kila kiumbe kilikuwa na furaha na amani. Hakuna kiumbe ambacho kilitaka kula kingine, kila kimoja kilikuwa kinamsifu Mungu na kuleta furaha kwa kingine. Mungu kama mzazi, alikuwa amebuni mengi ya kufurahisha viumbe Vyake. Ayubu 38:7 inasemwa baada ya uumbaji nyota za asubuhi ziliimba pamoja na wana wote wa Mungu walio nje ya dunia yetu walipiga kelele kwa furaha.

Mwanadamu alipaswa kubeba sura ya Mungu, katika kufanana Naye kwa nje na kwa tabia. Kristo peke Yake Ndiye 'mfano dhahiri' (Waebrania 1:3) wa Baba; lakini mwanadamu aliumbwa kwa sura ya Mungu. Asili yake ilikuwa ni ya upatanifu na mapenzi ya Mungu. Akili yake ilikuwa na uwezo wa kufahamu mambo ya Bwana. Mapenzi yake yalikuwa safi; matamanio na shauku zake yalikuwa chini ya udhibiti wa akili. Alikuwa mtakatifu na mwenye furaha na mwenye kubeba sura ya Mungu, katika utiifu mkamilifu kwa mapenzi Yake yote. Mwanadamu aliumbwa mkamilifu na bila hatia, alipewa uchaguzi wa kuchagua, hakuwa roboti au mashine inayoamrishwa kufanya kila kitu!

Mwanamke inampasa kuwa kama kanisa, na mwanamume kama Kristo. Mwanamume ameagizwa na Mungu kumpenda mkewe, na mke ameagizwa kumtii mumewe. Hii ni amri, ya Mungu haina mijadala, mume afanye yote yampasayo ili kufanya ndoa yake kuwa bora na mke naye afanye yote yampasayo ili ndoa yake iwe bora, na hilo litafanya nyumba zetu ziwe kama mbingu ndogo hapa duniani. Kila aliye katika ndoa anapaswa kujifunza kuishi katika ndoa, na katika familia!

Hatuzaliwi tukiwa tunajua la kufanya. Utafiti ulionyesha kwa wabaptisi Marekani kwamba asilimia 50% ya ndoa huvunjika, ila wale wanaoomba pamoja, maombi ya dhati na bidii, ambayo si feki/bandia, ni ndoa moja kati ya 1023 huvunjika!

*Wazazi wamewaleta watoto katika ulimwengu ambao hawakuwa na sauti au maamuzi kuhusiana na uwepo wao. Mmejifanya wenyewe kuwajibika kwa kiwango kikubwa kuhusu furaha yao ya baadaye, na ustawi wao wa milele. Jukumu liko juu yenu, iwe mnalihisi hili au la, kuwafundisha na kuwalea watoto hawa kwa MUNGU, kuwatunza kwa uangalifu wenye wivu mara tu adui mjanja anapotokezea na kuweka hatua yake ya kwanza, na kisha muwe tayari kuinua kiwango dhidi yake. Jenga ngome ya maombi na imani juu ya watoto wako, na ufanye bidii kukesha humo. Hauko salama hata kidogo dhidi ya mashambulio ya Shetani.

---

Kwa nini Mungu alimwumba mwanadamu? Mwanamume wa kwanza aliitwa nani? Mwanamke wa kwanza aliitwa nani? Bustani waliyoishi iliitwaje? Orodhesha mambo kumi yanayofanya ndoa iwe bora.

**SIKU YA 3**
**(January 3)**

# Siku ya Saba na ya Mapumziko kwa Binadamu

**- *Mwanzo 2***

Wazazi huwaza jinsi ya kuleta furaha na amani kwa watoto wao. Mungu aliweka pumziko kwa binadamu ili ampatie furaha na amani. Siku ya saba, Mungu aliacha kazi Yake na kupumzika. Kwa Kiebrania inaitwa Sabato, yaani siku ya pumziko. Tunapata siku 365 za mwaka kutokana na dunia kulizunguka jua, na siku 28 kutokana na mwezi kuizunguka dunia, bali siku saba ndizo zinazofanya juma, yaani juma moja lina siku saba. Siku sita za kufanya kazi na siku ya Saba ya kupumzika. Siku ya saba imewekwa kukumbuka uumbaji kwamba sisi tu viumbe na tunaye Muumbaji. Hii inatusaidia tuepukane na nadharia ya mabadiliko ya viumbe toka viumbe sahili na kuwa na mifumo tata au mafundisho ya aina hiyo. Katika siku hii ya saba Mungu alipumzika, akaibariki na kuitakasa. Itakuwa aliwaambia siku ya sita kuhusu siku hii, kwamba ni takatifu (imewekwa wakfu). Siku hii ilitolewa iwe siku ya kupumzika na kuzungumza Naye. Aliwapatia Adamu na Hawa siku hii kama zawadi. Mungu hachoki, ila tunaambiwa alipumzika! Adamu na Hawa walikuwa hawajachoka maana walikuwa hawajafanya kazi yoyote, bali aliwapa siku hii kuwa na mawasiliano rasmi naye. Alichukua muda kuzungumza nao. Walizungumza na Mungu uso kwa uso! Hawakutunza Sabato tu bali waliisherekea. Pengine walizungumzia uumbaji, pengine aliwazungumzia sayansi ya kupumua kwa mamba au jinsi nyuki anavyotengeneza asali. Walijifunza mengi moja kwa moja toka kwa Muumba wao. Alisema kuwa alifanya siku hii ya Sabato kwa ajili ya mwanadamu. Katika bustani ya Edeni, Mungu aliwapatia Adamu na Hawa kazi ya kufanya, ndoa na mapumziko ya siku ya saba ya juma, yaani Sabato. Hata leo, baada ya miaka 6000 watu wanabarikiwa kwa kutunza siku hii ya Bwana au Sabato takatifu. Vitu vyote ambavyo viliumbwa kwa siku sita vipo, yaani, Mwanga, anga, mimea, mianga ya jua, nyota na mwezi, wanyama, na binadamu tunayo hata leo, hayajatokomea. Vivyo hivyo Sabato tuliyopewa siku ya saba bado ipo, Mungu hakuiondoa.



Mungu alipowatoa Waisraeli katika utumwa kule Misri, aliwapatia Amri Kumi na kuwakumbusha juu ya Sabato katika amri ya Nne inayosema, "Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase, siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba, kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya sabato akaitakasa". Amri hii ndiyo pekee inayosema "ikumbuke". Aliona wengi watatingwa na shughuli nyingi hata kusahau siku ya kuwasiliana na Mungu. Sabato ni ishara ya agano la Mungu na wanadamu. Tunafundishwa kutunza Sabato jinsi inavyotakiwa katika Isaya 58; yaani, kujiepusha na anasa zetu na kushugulikia wenye shida na mahitaji. Mungu ametupatia siku sita za kufanya kazi na kutende mambo yetu. Hii ina maana tusiwe wavivu bali tuwe watu wenye bidii kwa kazi zetu katika siku hizo sita. Kristo alipokuja duniani Naye aliendelea na pumziko la Sabato - Luka 4:16. Usiendelee kufanya shughuli zako za kila siku. Mungu amekupatia siku sita, lakini ya saba ni Yake, maalum kwa ajili ya kumwabudu na kuwasiliana Naye. Hata kule mbinguni watu watasherekea siku hii Isaya 66.

Mungu aliumba miti mikubwa. Aliumba wanyama wakiwa wa umri wa mnyama mkubwa. Adamu na mkewe waliumbwa pia kama watu wazima. Bustani ilipendeza na walitembea bustanini wakiifurahia na kuzungumza na Muumba wao katika siku hii ya saba. Nafikiri waliikumbuka maisha yao yote baada ya kuanguka. Ilikuwa siku ya kushangilia uumbaji. Mungu hakuwajengea jumba la usultani, japo Adamu alikuwa mfalme wa dunia, na mkewe alikuwa ni malkia. Aliwapatia bustani, na siyo ghorofa, au nyumba ya umeme. Kuta za nyumba zilikuwa miti mizuri, na maua. Mazulia yalikuwa majani yenye kupendeza. Hakukuwa na haja ya kujikinga na vitu vinavyoanguka, wezi, au mvua. Walilala nje, wakifurahia sauti tamu za ndege. Hawakuhitaji sahani za kuwekea matunda! Ilikuwa furaha kubwa. Hakukuwa na haja ya kupika, au kiwanda cha masufuria. Hili nalingojea kwa hamu mbinguni! Najua hawakula kwa ulafi au siku nzima, walitenga muda maalum wa kula. Walizungumza pamoja. Pengine Hawa alisema, "Adamu angalia ua hili zuri". "Hawa angalia simba". Pengine, walifika kwenye miti miwili ya kati ya bustani, "mti wa uzima na mti wa kujua mema na mabaya". Mungu alikuwa amewaagiza kwamba miti mingi iliyokuwepo, yote wanaweza kula matunda yake, ila matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya "msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. "Kufa?" Bila shaka walijiuliza kuwa maana yake ni nini, maana walikuwa hawajaona aliyekufa. Pengine walijiuliza kwanini Mungu ameumba mti ule. Waliendelea kutembea na kufurahia uumbaji. Mungu alimwumba mtu kwa mfano wake, na siku ya Sabato ilikuwa ya mahusiano naye. Jua lilipotua walifurahia, uumbaji umekamilika, Mungu ametimiza lengo lake la upendo. Hata leo, tenga siku hiyo kwa BWANA uwe na mahusiano naye, uache shughuli zako za kawaida za kila siku, maana zenyewe haziishi, hasa katika dunia ya leo! Iwe kupika, kusafisha viatu, kushona vifungo nk. Mtu ndiye huchakaa, boresha na rejesha afya siku hii moja ya wiki.

Sabato ingetunzwa MUNGU alivyokusudia baada ya uumbaji na katika maandiko kama vile Isaya 58, Siku iliyotengwa na kutakasa kusingekuwa na

mtu mmoja aliye mpagani au kafiri. Kwani watu wote wangekumbuka ni siku ya muhimu ya mahusiano na MUNGU Muumbaji aliyewaumba wao. Ilikuwa sikukuu ya kusherekea uumbaji wa MUNGU. Wengi wamesema ni ya Wayahudi. Jambo hili si kweli kwani Sabato iliwekwa miaka 2300 kabla ya Wayahudi kuwepo. Wayahudi wa kwanza ni wajukuu wa Ibrahimu. Adui hapendi tukumbuke kwamba sisi ni viumbe tulioumbwa na MUNGU, anapenda tusahau na kwa miaka mingi ameleta machafuko mengi ya kufanya sabato isahauliwe. Sabato ni ishara kati yetu na MUNGU ili tujue YEYE Ndiye atutakasaye, na kwamba ni BWANA na MUUMBA wetu. MUNGU baadaye akaandika Amri Yake kwenye mawe na si mchanga. Amri kumi kwa mkono Wake Mwenyewe nayo ilisema “Ikumbuke siku ya Sabato uitakase”. Alijua kwamba binadamu atasahau.

*Hebu wazazi wamtafute MUNGU kwa ajili ya mwongozo katika kazi zao. Wakiwa wamepiga magoti mbele Yake watapata ufahamu wa kweli wa wajibu wao mkuu na huko wanaweza kuwakabidhi watoto wao kwa Yule ambaye hakosei kamwe katika ushauri na mafundisho.

---

Maswali: Kwa nini Mungu aliweka siku ya mapumziko? Siku hii ilikuwa siku ya ngapi ya juma? Mungu alifanya nini siku hiyo? Je, wewe una matayarisho gani katika siku hii kukutana na Muumba wako? Kwanini shetani hapendi tukumbuke Sabato? Je! Nitajuaje kwa hakika kwamba ni siku gani ya juma? Je, Unaweza kusema siku uliyozaliwa ni jumapili wakati ni jumamosi?, MUNGU alitoa zawadi nne wakati wa uumbaji, je zawadi hizi zilikuwa zipi?



**SIKU YA 4**
**(January 4)**

# Anguko la Mwanadamu-Jinsi Dhambi Ilivyoingia na Mapambano yalivyoanza hapa Duniani-

**Mwanzo 3**

Mwanzo moja na mbili inaeleza kuhusu uumbaji. Mwanzo tatu inaeleza kuhusu anguko, na sehemu ya Biblia iliyosalia inaeleza urejeswaji baada ya anguko. Kama Baba mwema kupita wote, bila shaka Mungu aliwaeleza vizuri kuhusu utii, kuishi milele, uasi na kifo. Amri Zake ni muhimu mno, hasa kwetu! Huenda hutapendezwa na mtu anayevunja Amri za Mungu. Anaweza kuua watu, atakupiga, atadanganya, na orodha hiyo ya maovu unaweza kuiendeleza! Ila Mungu alimpa mtu uchaguzi, huu unasaidia mtu kupevuka vyema, kuwa na upendo wa dhati na siyo kuwa kama roboti, mtu akishinda kwa kuchagua vyema, huweza kuwa na mahusiano ya karibu sana na Mungu, kwa vile amekuwa huru kufanya uchaguzi wake.

Bila shaka siku hizo ambazo Adamu na mke wake walikaa kwenye bustani ya Edeni zilikuwa za furaha kubwa. Ufalme wote ulikuwa wao. Walitembea kama mfalme na malkia, wakimiliki kila kitu! Walikuwa hawana shida au mahangaiko. Kulikuwa hakuna huzuni, kulia, maumivu au kifo. Hebu mtoto piga picha akilini mwako, siku isiyokuwa na maumivu ya meno, magomvi, njaa, kifo au ugonjwa. Maisha yao yalikuwa na ubora usio na kifani. Kutunza bustani kulikuwa hakuwatoi jasho bali kulileta furaha na mazoezi ya mwili. Hapakuwa na miiba wala magugu ya kupalilia. Lakini kutotii kuliharibu yote hayo kwa siku moja tu.

Siku moja Adamu na Hawa walipokuwa katika shughuli zao bustanini, Hawa alitaka aungalie ule mti wa kujua mema na mabaya. Mti ule wa ajabu uliokuwa bustanini. Alianza kujiuliza ni kwa nini Mungu aliwapa Maagizo hayo? Kujua mema na mabaya kuna maana gani? Kwa nini asile matunda yale? Mungu alikuwa ametoa zawadi ya kila kitu, isipokuwa tu kile alichoambiwa siyo chao na Maagizo Yake yalieleweleka vyema. Waliruhusiwa kula matunda ya mamilioni ya miti! Miti hii inaweza kufananishwa na zaka au chochote kilichowekwa wakfu kwa BWANA. Vitu vilivyowekwa wakfu na BWANA havipaswi kuwa na matumizi zaidi ya yale aliyoagiza au aliyoamuru Mwenyezi MUNGU. Ukiangalia sana jaribio hili lingeweza kuepukika, kwasababu kulikuwa na miti mamilioni mingine ambayo angeenda kuzuru na asingepata shida. Yaonekana Shetani alipotupwa toka mbinguni hakuruhusiwa kutembea bustani yote isipokuwa kwenye mti huu tu! Hizi zilikukwa rehema za Mungu. Na hata kama mwanadamu angeamua kwenda pale, asingepaswa kukaa pale na kuanza kujibu maswali ya yule asiyemfahamu vizuri au aliye na mashaka naye. Na isitoshe hata kama angezungumza naye alikuwa na uwezo wa kukataa kula lile tunda. Basi hata leo tujiulize, Je! Kuna maovu gani



ambayo tunayaweza kuyaepuka kwa kuwa na hekima na kuomba MUNGU atusaidie tusiende kwenye vishawishi hivyo.

Basi Hawa alipogeuka kutembea alishangaa kuona kuwa kuna kiumbe kinazungumza naye. Viumbe vyote isipokuwa mtu, havikuzungumza. Akitazama aliona nyoka, mwenye sauti ya kuvutia na kuonesha urafiki ambao wazungu wanauita aduirafiki (frenemy). Badala ya kukimbia, alisimama pale akiwa na udadisi zaidi. Maskini, kumbe alikuwa ni Shetani ambaye anadanganya dunia nzima. Kwanza alijulikana kama Lusifa, yaani malaika wa Nuru, ila alitupwa toka mbinguni (Ufunuo 12), akiwa na chuki na hasira ya kulipiza kisasi kwa kuharibu furaha ya watoto wa Mungu. Hawa hakujua hili, la sivyo asingeanguka mtegoni, ila alikuwa ana uchaguzi wa kuamini Neno la Mungu au kufanya yake mwenyewe.

Nyoka akamwuliza Hawa "Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke akaanza kujibizana na nyoka bila tahadhari. Akasema, "Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula. Lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema msiyale wala msiyaguse". Nyoka akajibu "hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu mkijua mema na mabaya". Hawa akaona kwamba ule mti unafaa na unatamanika kwa chakula. Japo hakuwahi kula matunda hayo kabla ya hapo, macho yalimdanganya, ila si macho peke yake, bali alichagua kutomtii Mungu. Akaona kwamba yeye anaweza kufanya tu yale anayotaka bila kumtii Mungu Mtawala na Muumbaji aliyewapenda sana. Alikula lile tunda, kisha akampelekea mume wake Adamu naye akala. Wakafumbuliwa macho wote wawili na wakajijua kwamba wako uchi. Wakakimbia wakiona haya, wakashona majani ya mtini ili wajifanyie nguo kuficha utupu wao. Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu akitembea bustanini wakati wa jua kupunga. Basi Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia "uko wapi?". Na Mungu leo anatuita kule tunakojificha, ni Yeye anayetutafuta na si sisi tunaomtafuta! Adamu akajibu "Nalisikia sauti yako bustanini nikaogopa, kwa kuwa mimi ni uchi nikajificha". Mungu akamwuliza "Ni nani aliyekuambia ya kuwa u

uchi? Je, umekula wewe matunda ya mti ule niliyokuagiza usiyale?". Adamu alitupa lawama kwa Mungu na mke wake kwa kusema ni "huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami, ndiye aliyenipa matunda ya mti huo nikala". Mungu alipomwuliza mwanamke kwamba ni nini alichokifanya, alitupa lawama kwa nyoka "nyoka alinidanganya nikala". Yaonekana Adamu alifanya dhambi akijua fika. Pengine alimpenda mke wake sana kuliko Mungu, na kukosa imani ya kutambua kwamba Mungu ana uwezo wa kumpa msaidizi mwingine au kumtoa kwenye uovu aliotenda mke wake. Dhambi ni uasi wa sheria. Adamu na Hawa waliasi sheria ya Mungu. Adamu ambaye hapo awali hakuwa na hofu bali upendo kwa Mungu; akizungumza Naye uso kwa uso, akaanza kuwa na hofu tangu siku ile. Uhusiano wao na Mungu ulijeruhiwa. Uhusiano baina ya wanandoa hawa pia uliharibiwa, na ndoa nyingi leo zina changamoto kwaajili ya jambo hili, na inabidi turejee kwa Mungu ili aponye familia zetu. Mungu alikuwa amewaonya juu ya adui mwovu na laghai aliyetupwa kutoka mbinguni, lakini waliamua wasisikilize sauti ya Muumba wao.

Basi vita vilivyoanza mbinguni vikawa vimeingia hata hapa duniani. Baada ya kuhamia hapa duniani, Shetani hakuweza kuwa mkazi wa kule mbinguni tena, maana alitupwa huku chini. Ila yupo hapa akitesa au kusumbua watu kwa njia mbalimbali. Yawezekana alienda kusumbua wakazi wa kila sayari yenye viumbe hai, nao wakamshinda. Twaambiwa kwamba kwenye rekodi au kumbumbukumu, vita vifupi kuliko vyote duniani, vilipigwana hapa kwetu Zanzibar kwa dakika 38 tu, mwaka ule wa 1896 kati ya Uingereza na Sultani wa Omani. Sultani wa Omani alijisalimisha na Waingereza wakakichukua kisiwa hicho kuwa chao. Na vita virefu kupita vyote vilianza kule mbinguni kati ya Shetani na Mungu navyo vimeendelea kwa miaka 6000 takribani sasa. Wewe na mimi na kila binadamu tunahusika. Vita hivi karibu sana viishe. Tunashauriwa tuvae silaha saba katika Waefeso sita ili kushinda vita hivi. Tafadhali soma Maandiko Matakatifu na ukiweza kukipata kitabu kinaitwa Pambano kuu kati ya Mungu na Shetani kisome, ili uweze kushinda vita hivi vyenye zawadi kubwa inayowangoja wale wote watakaokuwa washindi kweye vita hivi, kwa msaada wa Mwenyezi Mungu.

Je, haitakuwa msiba wa kutisha zaidi, ikiwa licha ya yote ambayo tumepitia chini ya Shetani, watu bado wanabaki katika utumwa wake? Lakini kuna haja ya sisi kuwaeleza suala hilo. Hii ina maana kuwahubiria injili. Kila Mkristo ni mjumbewa Mungu aliyebahatika kusikia habari hizi njema. Tuifanye kazi hii kwa haraka inayostahili.

Shetani ni mwongo. Kupitia udanganyifu wake ubinadamu alitumbukizwa katika taabu na maumivu. Mungu ameturehemu sana, ametupa nafasi ya pili, tuchague uzima. Mungu anahitaji utii na kujisalimisha kwetu, haitaji maoni yetu! Akisema kwamba zaka ni asilimia kumi, au siku ya Sabato ni ya kutunzwa basi anamaanisha hivyo! Akichukua maoni ya kila mtu unafikiri maisha yetu yatakuwaje? Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Kwa maana Mungu hakumtuma Mwana Wake ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika Yeye.

*Kwa maombi ya dhati na ya bidii wazazi wanapaswa kuwawekea ulinzi watoto wao. Wanapaswa kuomba kwa imani kamili kwamba MUNGU atakaa pamoja nao, na kwamba malaika watakatifu watawalinda wao na watoto wao dhidi ya nguvu katili za Shetani.

---

Je, kulikuwa na miti mingapi pale bustanini? Mti ambao walikatazwa wasile uliitwaje? Nyoka alikuwa mwerevu na alimdanganyaje Hawa? Adamu alijuaje kwamba yupo uchi? Je, Hawa kumsikiliza nyoka ingekuwaje? Unafikiri Adamu na Hawa walijisikiaje? Unafikiri Mungu alijisikiaje? Je, kwa nini mwanadamu anapaswa avae nguo za kumsitiri vizuri leo? Somo hili linakufundisha nini kuhusu utii leo hapo ulipo?

**SIKU YA 5**
**(January 5)**

# Shetani Aanguka Toka Mbinguni - Ufunuo 12, Ezekieli 28, Isaya 14, Yohana 3:14-20 na Ayubu 1.



Neno la Mungu linatuambia kwamba Shetani alikuwa malaika mbinguni, jina lake aliitwa Lusifa, nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi. Lusifa ndiye aliyekuwa mwaanzilishi wa dhambi. Kitabu cha Ezekieli kinamfananisha Shetani na mfalme wa Tiro. Alikuwa ndani ya Edeni bustani ya Mungu, kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chake, dhahabu, almasi, yakuti, yaspi, n.k. Kazi ya matari yake na filimbi zake zilikuwa ndani yake, katika siku ya kuumbwa kwake zilitengenezwa tayari. Yeye alikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye. Mungu alimweka akawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu. Shetani alionekana mkamilifu katika njia zake toka siku alipoumbwa mpaka uovu ulipoonekana ndani yake. Alijazwa udhalimu na kutenda dhambi, na kwa sababu hiyo Mungu alimtoa kwa nguvu toka mbinguni na kumtupa chini. Fahari yake ikashushwa, na sauti ya vinanda vyake. Moyo wa Shetani uliinuka kwa kiburi kwa sababu ya uzuri wake, akasema "Nitapanda mpaka mbinguni, nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu, nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano." Alitaka kufanana na Yeye Aliye juu, yaani Mungu, akitaka aabudiwe na viumbe wafuate masharti yake. Lakini alishushwa. Uzuri wa kuonekana usijenge kiburi ndani yetu hata tufanye dhambi. Inaonekana pia alikuwa mwimbaji mzuri, haya yote yalimfanya awe na kiburi kwa kutosikiliza Maagizo ya Mungu, na akafanya uasi mbinguni. Hebu Mungu atusaidie ili tunapokuwa na talanta fulani, isilete kiburi ndani yetu na badala yake tushukuru kwa unyenyekevu, tukimpatia Mungu utukufu maana Ndiye mpaji wa vyote. Hata kwenye kujipamba ni vyema kuwa waangalifu. Vito vyote vya thamani, Mungu alimwumbia binadamu. Ila binadamu amechukua vito na kuvivaa kwa kujionesha au kuleta kiburi. Adui huyu sasa amekuwa kama simba angurumaye akitafuta watu awameze.

Mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele. Kama wanadamu, dhambi imeingia kwetu sote kupitia wazazi wetu. Adamu na Hawa waliendelea kujiuliza tena na tena maana ya Maneno ya Mungu kuwa, "nitaweka uadui kati yako na mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake, huo utakuponda kichwa, nawe utamponda kisigino". Hawakujua Maneno haya ni baraka ili wasimpende Shetani sana na kuchukuliwa moja kwa moja. Mungu aliwapa tumaini kwamba siku moja watapata mkombozi. Nao walifikiri pengine wangerudi tena Edeni. Pengine walifikiri mtoto wao wa kwanza (uzao wa mwanamke) atawaokoa kutoka kwenye shida ile. Mungu aliposema uzao wa mwanamke pale Edeni alikuwa ana maana ya Imanueli, au Mungu pamoja nasi au Kristo atakuja awaokoe. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika Yeye". Pale penye ulimwengu, weka jina lako. Hata ingekuwa ni wewe tu Mungu angekuja kukuokoa. Mungu ni upendo, apenda watu. Mungu hakutaka kuwakatisha tamaa kwa kuwaambia itachukua maelfu ya miaka. Watu wengi siku hizi wanacheza na Shetani kama hawa alivyofanya. Mfano: kwa kusoma vitabu vya uchawi kama Harry Porter au Wica. Wengine wanaamini kuwa 'Shetani hayupo'. Usipomjua adui yako, umepoteza pigano. Shetani yupo, Neno la Mungu linaeleza wazi. Baadhi ya mataifa wana siku za kusherekea wachawi, wakifikiri ni mchezo, kwamba kuna "wachawi wazuri na wabaya". Hili ni kosa. Shetani ni kiumbe aliyeumbwa kama malaika wa nuru, lakini aliasi, hana jema. Kwa sasa anangoja adhabu yake siku ya mwisho, lakini anataka adanganye binadamu ili aangamie nao. Adhabu ya Jehanamu haikuwa ya binadamu ila ni ya Shetani na malaika zake. Tuombe Mungu atupatie nguvu ili tujinasue mitegoni mwa Shetani na tuipate Paradiso, yaani, kwenda mbinguni.

Jambo la muhimu kuelewa ni kwamba tupo kwenye mapambano makali, kati ya wema na ubaya au Shetani na Mungu. Tunajiuliza, mbona hatuoni makombora yakitupwa au bunduki zikilia? Ah! Mapambano haya yamo kichwani! Sauti mbili zinasikika kila dakika, nichague hili au lile. Sauti ya Malaika wa Mungu na sauti ya malaika wa Shetani. Roho wa Mungu anazungumza na dhamira zetu kila dakika. Tufanyeje basi? Soma Waefeso 6 vizuri. Inatutaka tuvae silaha za Mungu tupate kuzipinga hila za Shetani na majeshi yake, kwa maana mapigano yetu si ya nyama na damu, bali ni dhidi ya falme na mamlaka za giza, majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Tujifunge mikanda viunoni, tujifunge dirii ya haki kifuani, viatu vya utayari wa injili, ngao ya imani, chapeo ya wokovu na upanga wa Roho kwa maombi tukikesha na kusali. Neno la MUNGU tulitafakari usiku na mchana kama YESU alivyoshinda majaribu alipokuwa duniani. Soma zaidi kwenye Mathayo 4.

Kitabu cha Ayubu kinatupatia picha kwamba zamani Shetani aliruhusiwa kutembea mbinguni akiiwakilisha dunia, "Natoka katika kuzunguka zunguka duniani, na katika kutembea huku na huku humo". Kitabu hichi kinatuambia pia kuwa mambo mabaya humpata mtu aliye Mwema. Pengine ziara hizi zilikoma wakati YESU aliposhinda na kuwa mwakilishi wetu! Waweza kuangalia zaidi kwenye mtandao kuhusu Theodicy of love by John Peckham kuhusu wema wa Mungu, na kwanini anaruhusu watu wengine waendelee kuteseka. Kwa kifupi Mungu Naye



anaendelea kuteseka watoto Wake wakiendelea kutendeana uovu, na kwamba adui yetu Shetani anataka kumwumiza Mungu kwa kupitia watoto Wake. Basi waumini wote "tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu". Mungu anataka kututumia na Shetani anataka kututumia. Shetani analazimisha kwa nguvu, Mungu anatoa uchaguzi.

*Wazazi, Je! mnafanya kazi kwa bidii isiyochoka na uvumilivu kwa niaba ya watoto wenu? MUNGU wa mbinguni anaona kujali kwako, kazi yako ya bidii, kukesha katika ulinzi kwako jwa kila wakati. Anasikia maombi yako. Kwa uvumilivu na upole wafunze watoto wako kwa ajili ya Bwana. Mbingu yote inapendezwa na kazi yako. Malaika wa nuru wataungana nawe unapojitahidi kuwaongoza watoto wako kwenda mbinguni. MUNGU ataungana nawe, akiwekea taji juhudi zako kwa mafanikio. Kristo anafurahi kuiheshimu familia ya Kikristo; kwa kuwa familia kama hiyo ni ishara ya familia iliyo mbinguni.

---

Je, Shetani yupo wapi? Ni nani mtenda dhambi wa kwanza? Shetani ana majina mengi, taja sita unayoyajua? Shetani alipotupwa toka mbinguni alianguka na malaika wangapi? Kitabu cha Ayubu kinatusaidia kujua jambo gani?

**Sura ya 6**
**(January 6)**

# Adhabu ya Uasi

**Mwanzo 3**

Adamu na mke wake walishindwa mtihani au jaribu. Wakafanya dhambi, hata sisi leo tunajaribiwa kila siku na kuingia dhambini au kushinda. Inatupasa tumwombe Mungu kila siku ili atusaidie kushinda. Na pale tunapokosea tumwombe msamaha na kwa toba ya kweli tufanye masahihisho. Imetupasa tujifunze kuwa na tabia Yake Mungu. Adui Ibilisi anakuja na majaribu mbali mbali kwa kusikia, kutenda, kunena, na kuwaza. Yaweza kuwa ni kiburi, tamaa mbaya, kukata tamaa, unafiki, chuki, wivu, kuwa mtu wa dunia anayependa anasa, au kuwa kafiri asemaye “hakuna Mungu”.

Je! Mungu alikuwa dhalimu kwa Adamu na Hawa? La! Hasha. Alikuwa amewapa uchaguzi wa kufuata sheria ili waishi kwa amani na raha au uasi na kuishi kwa huzuni. Je, waweza kujadili na wazazi wako, nchi isiyo na sheria ina shida gani? Je, usipotii sheria za asili itakuwaje?



Mungu aliwapa mavazi ya mwanakondoo, badala ya majani yaliyokuwa yameficha utupu wao nusu nusu. Pengine hii ilikuwa ni kafara ya kwanza, ili wavikwe vazi la Haki ya Mungu. Pia Hii inaonesha kwamba si vizuri kuvaa nusu nusu bila adabu, kwani Mungu alitupatia nguo zitufunike vizuri - kusitiri aibu, baridi, na joto. Usidanganyike kuvaa nguo nusu nusu kama zile za majani ya mkuyu, eti zipo kwenye fasheni, Mungu angetaka tuvae vile asingewatengenezea Adamu na Hawa nguo za heshima za kuficha utupu wao.

Bwana Mungu akamwambia nyoka, kwa sababu umefanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko wanyama wote, kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako. Nami nitaweka uadui kati yako na mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake (watoto wako na watoto wake).

Uzao wa mwanamke utamponda kichwa nyoka, na nyoka atakiponda kisigino cha uzao wa mwanamke. Nyoka toka siku hiyo akawa adui ya binadamu. Tukimwona tunamuua, akituwahi anatuuma, pia hutambaa kwa tumbo na wala hatembei. MUNGU kuweka uadui kati yetu na Shetani ni jambo jema, kwani ni ahadi ya pekee na neema kubwa la sivyo tungemwona shetani ni rafiki na angetuangusha vibaya sana.

Kisha Bwana Mungu akamwambia mwanamke "hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako kwa utungu utazaa watoto, na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala." Mahusiano kati ya mke na mume pia yakaanza kuwa magumu. Basi Wanamume ambao hawawapendi wake zao, na wana utawala waliopewa na Muumba wakaanza kuwatesa na kuwanyanyasa wake zao, watoto wao na wote walio chini ya mamlaka yao kama wanyama. Kuzaa haikupasa kuwe ni kwa uchungu, lakini wakina mama wengine wakikusimulia maumivu yao utashangaa, hata wengi wamepasuliwa, wamepasuka au wamekufa wakati wa kujifungua. Mama mmoja alisema mtu akiwa mjamzito katika kabila lao wao husema "mguu mmoja upo duniani na mwingine kaburini". Hii yote ni adhabu yetu binadamu kwa kutotii Maagizo ya Mungu. Wengi wamesema wakina Hawa wametuingiza kwenye shida, ila hata leo ule uchaguzi waliokuwa nao, tumepewa pia. Je, tunamchagua Mungu na njia Zake au tunamchagua Shetani? Je! Tunamtilia Mungu mashaka na kujifanyia tunachokitaka?

Mungu Akamwambia Adamu, "kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nilikuagiza, nikisema; usiyale, ardhi imelaaniwa kwa ajili yako, kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako. Michongoma na miiba itakuzalia nawe utakula mboga za kondeni. Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi."

Lo! ilikuwa siku ya huzuni kubwa kupita zote duniani. Nafikiri walitishika na kutetemeka kwa hofu. Dhambi inaleta hofu kubwa. Badala ya kufanya kazi kwa furaha na kwa urahisi, ikawa ni kufanya kazi kwa nguvu, na huzuni, na mara zingine bila hata mavuno yoyote kwa ajili ya ukame au shida zingine za dhambi. Nafikiri walipoanza kuona majani yanakuwa ya njano, yanakufa na kuanguka, walilia machozi. Waliona wanyama wakifukuzana na kulana. Sote tumeshawahi kukanyaga miiba, na tunajua maumivu yake. Dhambi ilileta huzuni mbinguni na sasa ilileta huzuni duniani. Mungu Naye alikuwa na huzuni kuu, giza la dhambi, lilikuwa limeingia. Usiku ulikuwa unaingia na walijiuliza waende wapi? Malaika pia walikuwa na huzuni, maana mbinguni huko kulishakuwa na shida ya dhambi, na sasa ilikuwa imeingia duniani. Hata wanyama pengine walihisi hofu na huzuni hii walipoona Adamu na Hawa wakilia kwa huzuni. Walifukuzwa kwenye bustani ya Edeni na Makerubi (malaika) waliwekwa kuilinda bustani hii kwa upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima. Mungu aliwapenda na kuwaonea huruma, hakutaka wale tena tunda la mti wa uzima, wakaishi milele, bali kwa huzuni kuu. Waligeuka waiangalie tena maskani yao waliyoifurahia, bustani iliwekewa wigo na geti lilifungwa. Dhambi ina gharama kuu isiyo na kifani. Adamu aliishi miaka 930 akafa, Pengine alitembea na kuonyesha uzao wake bustani ambayo alifukuzwa. Akawasihi wamtii Mungu, akiwalezea raha waliyokuwa nayo

kabla ya dhambi. Hata hivyo, watu wengi hawajifunzi kutokana na uzoefu wa wengine. Wanapenda wapate adhabu zao wenyewe, hivyo hufanya majaribio yanayoleta huzuni. Inasemekana kuwa Bustani hii ya Edeni ilikaa miaka mingi pale Iraki. Inawezekana kwamba Mungu aliichukua kabla ya gharika ambayo ilikuwa mwaka 2348 hivi KK (Kabla ya Kristo), ukijumlisha miaka ya vizazi vya Adamu.

Unaweza kujiuliza leo hivi hawa binadamu walianzaje kula tunda lililokatazwa hadi kufikia kuua wengine? Sheria za Mungu zinashikamana zote, ni kitu kimoja kama bilauri, ikivunjika kipande chake basi zote zimevunjwa. Hakika kuelezea dhambi ni kuitolea udhuru, dhambi haina sababu ya kutokea, na haina maelezo, ni fumbo la ajabu kwamba lilitendwa, hasa ukifikiria kwamba Mungu ana Upendo wote kwetu. Si Kaini pekee aliyemuua Abeli, Lameki pia alimuua kijana. Maelezo ya mauaji hayo hayajafichuliwa, lakini yalihesabiwa kuwa yanafaa kuadhibiwa, mara kumi zaidi ya Kaini alivyostahili adhabu. Kwa hivyo, tunaona hapa vizazi vinavyofuata vya ubinadamu vikiendelea kuwa vibaya zaidi. Siku hizi makombora mazito yanauta watu mamilioni kwa muda mfupi! Hakika tunakaribia nyumbani. Mungu aliwaeleza mpango wa wokovu, na jinsi bustani ya Edeni au Paradiso itakavyorudishwa tena, kupitia kifo cha Mwana Wake. Tujifunze kumwamini Yesu na kumtii ili tuweze kuwa katika paradiso mpya. Mama aliye na miaka 90, aitwaye Gloria kwenye darasa langu la Biblia, alinishauri na wanangu “Waafrika hakika tumepata shida nyingi, kuanzia utumwa, ukoloni, ukoloni mamboleo, na kisha kubaguliwa, kudharauliwa na kunyanyaswa kati ya mataifa ya dunia na kama hatutakuwepo mbinguni, basi itakuwa sikitiko na ujinga mkubwa, maana tutakuwa hapa duniani tumekosa na kule mbinguni tumekosa”. Nimekaa na kujaribu kuyacheua maneno yake kwa makini.

*Baba, au, akiwa hayupo, mama, anapaswa kuongoza ibada, akichagua sehemu ya Maandiko yenye kupendeza na kueleweka kwa urahisi. Huduma inapaswa kuwa fupi. Wakati sura ndefu inasomwa na maombi ya muda mrefu yakatolewa, huduma hufanywa kuwa ya kuchosha (kuboesha), na katika kumalizika kwake hisia ya kushusha pumzi ya afueni husikika. MUNGU huaibishwa na kukosewa heshima wakati saa ya ibada inapofanywa kuwa kavukavu na ya kuwakasirisha (kuwasumbua moyoni) wana familia, inapokuwa kama shuguli nzito sana, ikapungukiwa na shauku, kiasi kwamba hata watoto wanaiogopa kwa kuifikiria kabla hata hawajaitwa kuja kushiriki. Ushawishi wa mama anayeombana kumcha MUNGU utadumu milele. Anaweza kufa, lakini kazi yake itadumu.

---

Adamu, Hawa na Nyoka walipata adhabu gani? Kwa nini Mungu aliwafukuza bustanini? Nani alilinda bustani? Kwa nini dhambi inaleta huzuni? Kwa nini watu hawasikii ukiwaambia wasirudie jambo fulani baya?

**SIKU YA 7**
**(January 7)**

# Mtoto wa Kwanza na Kifo cha Kwanza, hakika hasira ni kitu kibaya sana

**- *Mwanzo* 4**



Adamu na Hawa walipojishonea nguo za majani, Mungu alikuja na kuwapa nguo za mwanakondoo, ambazo zinasitiri utupu na hali ya hewa. Siku hizi wengine, wanataka kutembea na nguo ndogo au fupi au za kukosa adabu. Wote tumepoteza utukufu wa Mungu na tunahitaji nguo kamili zitufunike. Hapa walianza kuelewa kwa kiasi fulani maana ya kifo, na jinsi ya kutoa kafara, wanapotenda dhambi, na kuomba msamaha. Kafara ilikuwa inamwakilisha Kristo "mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya dunia" Ambaye angekuja siku za usoni. Walielezwa vizuri jinsi ya kutoa kafara hii. Si kwa mazao ya mashambani, bali mifugo. Ilikuwa lazima damu imwagike, maana bila kumwagika dhambi hakuna ondoleo la dhambi Warumi 6:23. Waliendelea kuchinja wanakondoo na kutoa kafara kwa miaka mingi mpaka wakati Kristo alipozaliwa na kufa mwaka wa takribani 31 BK.

Adamu na Hawa walibarikiwa kupata mtoto wa kwanza wakamwita jina lake Kaini. Pengine walifikiri huyu atakuwa mkombozi. Walipata mtoto wa pili na kumwita Habili. Mungu aliwapa maagizo kamili ya jinsi ya kutoa kafara kwa ajili ya dhambi zao. Mwanamume ndiye aliyetoa kafara kwa ajili ya familia yake. Aliziungama dhambi zake na kisha akachinja mwanakondoo, ikilenga kifo cha Yesu "Mwana-Kondoo aichukuaye dhambi ya ulimwengu".



Kaini alikuwa mkulima na mdogo wake, yaani, Habili alikuwa mfugaji. Wote walileta kafara zao, Kaini alileta mazao ya mashambani. Hakutaka kusikiliza maagizo ya Mungu na kuleta kafara inayohitajiwa, bali Habili alileta wazao wa kwanza wa mwanakondoo. Mungu aliipokea sadaka ya Habili kwa kuiteketeza kwa moto, bali sadaka ya Kaini ya 'mazao' ilikaa vile vile kwenye madhabahu. Kaini alikasirika, sana na uso wake ukakunjamana. BWANA akamwambia kwa nini anafanya hivyo? Hata leo Mungu anaona tunapokasirika na kuwa na chuki au wivu kama Kaini. Alimkumbusha kwamba akitenda vyema atapata kibali, bali asipotenda vyema dhambi inamnyemelea mlangoni pake na inampasa aishinde. Badala ya kuomba kondoo kwa ndugu yake ili asahishe kosa lake, akajiona ana haki, na kwa hasira akaongeza uovu zaidi.

Kaini akamwambia nduguye Habili waende naye uwandani, naye akamwinukia ndugu yake akamwua. Hatujui alitumia silaha gani au wazazi walipataje habari. Biblia ni kitabu kilichoandikwa kwa muhtasari, kingeandika yote, makaratasi yasingetosha, wino ungeisha au hata watu wasingeweza! Inaonekana Kaini alikuwa na njia fulani za uovu. Basi walikimbilia uwandani na kuona mwili wa mtoto wao usio na uhai. Hawakujua kifo kina maana gani, walijaribu kumwita Habili, lakini wapi. Ndipo walipoanza kujua kwa mbali maana ya kifo, na kwamba dhambi yao kama wazazi ilikuwa na matokeo mabaya mpaka kwa watoto wao. Walilia mno kama Daudi alivyomlilia Absalomu, "Mwanangu Habili! Ingekuwa nafuu mimi nife badala yako mwanangu Habili". Nimefikiri huu ni wakati ambapo kulikuwa hakuna televisheni au uovu sana, Je, alipataje mafikara machafu haya? Nikagundua kuwa moyo ni mdanganyifu, na una ugonjwa wa kufisha. Mara zote tujikabidhi kwa Mungu, maana tusipofanya vile tutatenda ya kutisha mpaka tutajishangaa. Basi tuanguke magotini pa Mungu na kujinyenyekeza ili atutegemeze kwa mkono wake ulio hodari. Mungu alijua kwamba Kaini ana hasira na akampa onyo ili ajirudi lakini hakutii. Inawezekana hata yeye alishangaa alipoona Habili hanyanyuki wala kupumua.

Bwana alimuuliza Kaini, "yuko wapi ndugu yako Habili?" Kaini akajibu kwa ujeuri, "sijui, hivi mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?" au ni sawa na kusema, "usinisumbue, mimi si yaya wake". Mungu alijua alichokifanya, na akamwambia "umefanya nini? Sauti ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi". Kaini akapewa adhabu kwamba atakapoilima ardhi haitatoa mazao. Naye atakuwa mtoro asiye na kikao duniani. Kaini akaomba apunguziwe adhabu kwani aliona adhabu yake ni kubwa haichukuliki. Akaogopa akisema, "nitakuwa mbali na uso wako, nami nitakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani, hata itakuwa kila anionaye ataniua". Bwana akasema kila atakayemwua Kaini atalipizwa kisasi mara saba, akamtia Kaini alama ili kila amwonaye asije akampiga. Kaini akatoka mbele ya uso wa Bwana akakaa Nodi mbele ya Edeni. Ni kama Adamu na Hawa walikuwa wamepoteza watoto wote. Ilikuwa siku ya huzuni kuu kwa Adamu na Hawa walipoona kwamba mtoto wao amemwua mwenzake. Kwa kweli watoto wa kwanza hupendwa sana na wazazi, lakini Kaini akawa chanzo cha huzuni yao. Mtoto wao mzuri akawa muuaji wa kwanza. Kaini alikuwa amevunja amri ya sita inayosema "usiue", na kwa kiburi na hasira yake akazivunja zote tisa zilizobakia. Alama aliyopewa iliwakumbusha watoto au mke wake na waliona mshahara wa dhambi ulivyo mchungu ili wasifuate mfano wake. Wazazi walipoteza watoto wote wawili maana Kaini alimwasi Mungu na alienda kuishi mbali nao.

Kaini alitaka kupinga sheria ya Mungu, hakutaka kutoa kafara iliyotakiwa kuonesha kuwa yeye ni mkosaji. Alitaka kuonesha kazi za mikono yake na pengine, uwezo wake kujiokoa mwenyewe. Sura hii matokeo ya kutisha ya hasira isiyodhibitiwa. Hisia zisizozuiliwa za Kaini zilimpelekea kumuua Abeli ndugu yake. Kuna madhara makubwa wakati hisia zetu ziko nje ya udhibiti. Kaini aliiacha nyumba yake, na kutanga-tanga kama "mkimbizi na mzururaji." akimangamanga huku na kule. Maisha yake yalibadilika ghafla. Uchaguzi mbaya, hisia zisizodhibitiwa na mitazamo hasi huleta matokeo mabaya. Kileo chaweza kuchangia kufanya mawazo yetu yasithibitiwe pia. Uchaguzi mzuri, hisia chini ya udhibiti, na hisia chanya husababisha matokeo chanya. Maisha chini ya udhibiti wa Roho wa Mungu yanatayarishwa kukabiliana na hali yoyote inayotokea katika maisha kwa mtazamo wa utulivu katika kusudi kuu la Mungu. Bwana atusaidie tuweze kuwaombea kaka na dada zetu kwani sisi ni walinzi wao!

Kaini akaoa akapata mtoto akamwita Henoko, naye Henoko akapata mtoto akamwita Iradi, Iradi akamzaa Mehuyaeli, na Mehuyaeli akamzaa Methushaeli, Methushaeli akamzaa Lameki. Lameki ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kuwa na wake wawili, Ada na Sila. Walizaa watoto waliokuwa wafugaji, wapigaji vyombo vya muziki na wafua vyuma.

Nafikiri kama wazazi, Hawa na Adamu walipoyakumbuka maisha yao kwenye bustani, kabla ya kutenda dhambi, walilia kwa uchungu mkubwa, kwamba wao ndio walianza kuleta majanga haya kwa wana wao na ubinadamu. Waweza tu kupiga picha ya huzuni na machozi yaliyowabubujika wapendwa hawa walipokumbuka haya matukio na kuwasimulia wengine. Hatuhitaji kufanya makosa yetu wenyeweili tujifunze, hebu tujifunze kutoka kwao waliotutangulia na kuishi maisha ya kumtegemea na kumtii Mungu. Maana hata kama wao wasingelitenda dhambi,

bado wanadamu sote tumepewa uchaguzi wa kumtii Mungu au kutomtii.

*Endapo wakina mama wangetambua umuhimu wa utume wao, wangeshinda kwenye maombi ya siri, wakiwaleta watoto wao kwa Yesu, wakiomba baraka Zake juu yao, na kuomba hekima ya kutekeleza ipasavyo majukumu yao matakatifu. Hebu mama aboreshe kila fursa ya kuunda na kutengeneza tabia, mazoea na haiba za watoto wake. Hebu na atazame kwa uangalifu ukuaji wa tabia, akizuia mienendo inayojitokeza kwa ukubwa, akiwatia moyo wale walio na upungufu. Hebu afanye maisha yake mwenyewe kuwa mfano safi na mzuri kwa uongozi wake wa thamani.

---

Kwa nini siyo vizuri kutembea uchi, au na nguo zisizo na heshima? Kaini alifanya dhambi gani? Kwa nini alipewa alama? Utawezaje kuishi na kaka, dada au wazazi wako bila chuki, wivu au ugomvi? Hatuwajibishwi kwa uchaguzi wa kaka zetu ila tunawajibishwa na ushawishi tunaouweka kwao, jadili hili!



**SIKU YA 8**
**(January 8)**

# Maisha ya Henoko

**- Mwanzo 5-8**

Adamu alizaa mwana mwingine akamwita jina lake Sethi. Biblia haitaji majina ya watoto wa kike, lakini kulikuwa na watoto wa kike waliozaliwa na Adamu na Hawa. Adamu alimpata Sethi akiwa na miaka 130, siku zile watu walizaa wakiwa na umri mkubwa na pia waliishi muda mrefu. Adamu aliumbwa na Mungu aishi milele, lakini kwa sababu ya dhambi, aliishi miaka 930 tu. Aliumbwa akiwa mtu mzima. Kwa miaka kadhaa, hawakujua kuugua, na Adamu aliona vizazi vyake sita kabla hajafariki. Sethi aliishi miaka 912, na alimzaa Enoshi aliyeishi miaka905.

Nasaba zinaweza zisiwe sura za kuvutia kusoma kwenye Biblia lakini zimejaa mengi kwa mwanafunzi mwenye bidii na Maandiko. Tunaona watu waliishi miaka mingi. Hilo linafunua Ukweli muhimu kuhusu Mungu. Muumba wetu alipanga wanadamu waishi milele. Alituumba kwa nguvu fulani muhimu ambayo hata karne nyingi baada ya dhambi nguvu hiyo ilibaki. Hatujui wanawake waliishi muda gani. Labda waliishi zaidi ya waume zao kama ilivyo kwa wengi sasa. Mwanamke wa pili aliyetajwa kwa jina ni Sarai, mke wa Ibrahimu, na kisha Milka, mke wa Nahori



(Mwanzo 11:29). Kisha tunaona mitara ikiingizwa na Lameki aliyetoka katika nasaba ya Kaini. Majina yao ni Adah - ikimaanisha kujipamba na Zila - podo la ala za muziki au mchezaji dansi mashuhuri! Jingine tunajua dunia hii ina miaka mingapi kwa kusoma ukoo/nasaba! Dunia yetu ina takribani miaka 6000. Na tunajua fika Yesu alitoka kwenye ukoo gani kwa kusoma hizi nasaba! Na kwamba kumbe sisi sote tumetoka kwa Adamu na Hawa. Sisi ni ndugu wa babu mmoja! Na Muumbaji mmoja! Hiyo inatubidisha sisi kutendeana wema, yaani kuacha hiana ya aina yoyote. Twapaswa kufuata ramani ya maisha yetu ambayo ni Maandiko ili tusipotee katika safari yetu. Hadi kwa Nuhu tunapitia mlolongo usiokatika wa historia simulizi iliyopitishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Na akili zao hakika zilikuwa kali, kwani waliweza kuhifadhi habari kwa usahihi hata wakiwa wazee. Kutokana na haya yote tunaweza kuona kwamba tunayo rekodi ya kweli ya historia katika Biblia. Historia ambayo tunaweza kuiamini na inaendanana historia ya dunia yetu hii, maana hakuna historia kwenye vitabu kabla ya Mesopotamia.

Enoshi alimzaa Kenani ambaye aliishi miaka 910, mtoto wake Mahalaleli aliishi miaka 895,na mtoto wake Mahalaleli aliyeitwa Yaredi aliishi miaka 962. Mtu aliyeishi miaka mingi kupita wote ni Methusela, aliishi miaka 969. Lameki aliishi miaka 777 na Nuhu 950. Haya yote utayapata katika kitabu cha Mwanzo 5. Kama ukichora chati, utagundua kuwa wale mababu tisa waliotajwa waliishi muda mmoja na Adamu, yaani Adamu aliona wajukuu/vitukuu vyake vya vizazi kadhaa. Ni Nuhu tu ndiye hakumwona Adamu. Hii ina maana vizazi vyote hivi vilijua kuhusu uumbaji toka kwa Adamu na kuona bustani ya Edeni! Hawakuhitaji vitabu, kwa sababu walikuwa na kumbukumbu nzuri. Walikuwa watu wenye akili na kimo kikubwa. Adamu aliwaambia majaribu yao na mke wake na kuanguka kwao. Bila shaka, aliwaambia kuhusu tumaini la Mkombozi atakayekuja. Ukichora chati ya miaka ya wazee hawa, utaona mstari mmoja ni mfupi, huu ni wa Henoko, ambaye baba yake Yaredi, aliishi miaka 962 na mtoto wake Methusela aliishi miaka 969. Yeye aliishi duniani miaka 365 tu. Hii ni kwa sababu alitwaliwa na kwenda mbinguni. Watoto ni wa thamani kubwa kwa wazazi, na kule mbinguni hawatakuwa watoto wetu tena, bali kaka na dada!

Tunaweza kuuliza ni kwa nini Mungu alimtwaa? Naamini alikuwa akimpenda Mungu na kuzungumza Naye. Basi akampenda Mungu, katika nia na moyo wake kwa kina mno. Mchana na usiku alifikiri kuhusu Baba yake wa mbinguni. Hakuwa mchoyo, na mwenye kujifikiria, awekaye hasira au mawazo maovu. Mawazo maovu ni mabaya kwa mtoto wa Mungu. Ninaamini Mungu aliona mtu ambaye alikuwa anaakisi tabia ya Moyo Wake. Alitambua upana wau pendo wa Mungu baada ya kupata mtoto wake wa kwanza. Wazazi wengi wanajua upana wa upendo wa Mungu pale wanapokuwa wamepata watoto. Henoko akajua habari za furaha. Kwa kutembea na kuzungumza na Mungu, akajua mipango ya Mungu ya mbeleni! Henoko alioneshwa mambo ya siku za usoni, akasema "Tazama Bwana anakuja na watakatifu Wake maelfu maelfu" Yuda 1:14. Katika kitabu cha Waebrania 11:5 inasema "… alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu". Hii ni rekodi nzuri ajabu ya mtu kuiacha kwa watoto wake. Urafiki wake na Mungu uliendelea kukua, hata siku moja Mungu akasema, 'njoo Rafiki yangu ili tukae karibu, kwa mazungumzo matamu kwa maana walipatana sana! Je, nawe unapenda utembee

na Mungu kwa mawazo, matendo, na maneno? Hebu mruhusu Roho Mtakatifu aishi na kutawala moyoni mwako. Basi tukifanya hivi tunajua kwamba tutaendelea kutembea Naye mbinguni.

Jambo la kusikitisha ni kwamba wakati Henoko akitembea na Mungu, vitukuu vingi vya Adamu havikufanya hivyo. Walikuwa waovu na wenye ubinafsi, wakamsahau Mungu. Waligombana, na kuuana kama Kaini alivyomuua ndugu yake. Watu waliendelea kutenda uovu, wakimfuata Ibilisi ambaye ni kama simba mla watu. Pengine Adamu na Hawa walipowaonya waliona kwamba hawa wazee wanawasumbua, na hata hivyo 'wao wenyewe walishindwa', ni nani basi angeweza? Adamu aliona ulimwengu ulioumbwa vizuri na wa amani ukigeuka kuwa mahali pa kutisha, hili lilimfanya ajutie dhambi yake. Ni vigumu kuelewa mambo hayo yalitokeaje haraka hivyo baada ya uumbaji. Kwa kweli binadamu tu wasahaulifu na, ni rahisi kuingia dhambini tusipomjali Mungu. Hatuna wema wetu wenyewe, bali imetupasa kumwomba Mungu ili atupatie wema wa kweli wa moyoni.


Majina yote yalikuwa na maana mfano -Adam: "mtu au mwanadamu", Sethi: "aliyeteuliwa", Enoshi: "kufa," au "dhaifu", Kenan: "huzuni, Mahalal'el: "Mungu Mbarikiwa" Jared: "itashuka", Henoko: "kuanza" au "kufundisha", Methusela: "atakapokufa kutatokea uharibifu", Lameki: "kukata tamaa" au "maombolezo", Nuhu: "faraja" au "pumziko."

Wana wa Mungu si malaika ila binadamu wanaompenda Mungu. Ni mbinu ya Shetani kuwaangusha wacha Mungu kwa kuwafanya waoe na mtu asiyemwamini. Mungu Je, Shetani ameacha kutumia mbinu hiyo tunapokaribia mwisho wa ulimwengu? La! Hajaiacha. Onyo la Mungu ni muhimu leo kama zamani: "Msifungwe nira pamoja na wale wasioamini. Kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana ushirika gani kati ya nuru na giza? 2 Wakorintho 6:14.

*Mama anapaswa kuanza kazi yake kwa ujasiri na nishati/nguvu, akitegemea mara kwa mara msaada wa Bwana katika juhudi zake zote. Hapaswi kamwe kupumzika kwa kuridhika hadi aone katika watoto wake mwinuko wa tabia ya kwenda juu unaoeleweka, hadi wawe na lengo la juu zaidi maishani kuliko kujitafutia raha zao wenyewe.

---

Je, fundisho la kisa hiki ni nini? Mtoto wa tatu wa Adamu aliitwa nani? Henoko aliishi miaka mingapi? Je, alienda wapi? Mtoto wake aliitwa nani? Baba yake aliitwa nani? Jina Methusela lina maana gani?






**SIKU YA 9**
**(January 9)**

# Nuhu, Safina, na Gharika

**- Mwanzo 6-8**



Ikawa wanadamu walipozidi kuongezeka usoni pa nchi uovu pia ulizidi kuongezeka japo kizazi kwa kizazi walielezana habari za wokovu, na kwamba siku moja watarudi Edeni kama wataukubali wokovu. Basi watu wakajitwalia wake waliowachagua, kinyume na mpango wa Mungu, wakala na kunywa. Pengine walikula kwa ulafi, walifuja mali, kutojali wenye njaa na kula vyakula au vinywaji ambavyo haitupasi kuvitumia kama vileo au vyakula vya aina fulani. Inaonekana kuwa watu wakiishi pamoja kwenye miji, wanafundishana uovu kwa kiwango cha juu sana. Bwana akasema, "Roho Yangu haitashindana na mwanadamu milele kwa kuwa yeye ni nyama." Basi siku za mwanadamu zikapunguzwa kuwa miaka 120, na hata urefu wake pia ukapungua. Kila kusudi alilowaza mwanadamu lilikuwa baya na ovu siku zote. BWANA akajuta kumwumba binadamu. Jambo la huzuni kabisa kwamba Muumba wetu anajuta kwamba ametuumba. BWANA akasema "Nitamfutilia mbali mwanadamu niliyemuumba usoni pa nchi" na viumbe vingine, ila Nuhu alipata neema machoni pa BWANA. Nuhu alikuwa mtu wa haki na mkamilifu, naye alikuwa na watoto watatu Shemu, Hamu na Yafethi. Dunia iliharibika na kujaa dhuluma, na kila mwenye mwili alifanya maovu na kuharibu njia yake. Nuhu alikuwa mtu wa haki na alipata huzuni alipoona watu wanafanyiana ubaya mkubwa. Mungu akamwambia Nuhu kwamba ataiteketeza dunia kwa sababu ya dhuluma, hivyo ajenge safina ya mti wa mvinje. Akampa Maagizo ya kuijenga. Urefu, upana na kimo ulikuwa futi 600 x 100 x 60. Ukubwa wa meli hii ilikuwa kama meli za siku hizi (mfano ile ya USA pride of merchant ni futi 990 x 101 x 122 ina ghorofa 12 na ina wafanyakazi 1000 na inaweza kubeba wanajeshi 14,000).

Inavyoonekana, watu walijua haya yote kwa maana Nuhu alihubiri miaka 120 habari hii, na kila nyundo ilipopigwa kujenga safina, ilikuwa ni hubiri. Isitoshe Mtoto alizaliwa na akaitwa, "atakapokufa, gharika itakuja" yaani Methusela. Na kweli mwaka Methusela aliokufa, ndio ulikuwa mwaka wa gharika. Mungu alitoa kila onyo, bali walipuuza, ila inawezekana wengine walioamini walifariki kabla ya gharika. Watu walimsaidia Nuhu kujenga safina pengine kwa malipo au wema, walisikia habari hii tena na tena wakafanya mioyo yao kuwa migumu.



BWANA akamwambia Nuhu kwamba ataleta gharika na itaharibu kila kitu chenye pumzi na mwili juu ya nchi. Akamwambia Nuhu na wanawe pamoja na wake zao waingie kwenye safina. Safina yaonekana ilikuwa na dirisha moja, tu nalo lilikuwa juu kwenye paa, waliangalia wokovu wao utokao juu mbinguni pale! Mungu Akamwambia Nuhu akusanye chakula chao na cha wanyama, maana wangelikaa kwenye safina karibia mwaka mzima. Mungu akampa Nuhu Maagizo juu ya wanyama watakaoingia kwenye safina – wale najisi waliingia wawili wawili , dume na jike, na wale safi waliingia saba saba. Kwa mfano, nguruwe wangeingia wawili na mbuzi au kuku saba. Miaka hii 120 Nuhu alishuhudia uovu mwingi. Watu walikosa huruma na kuuana, na palikuwa na maumivu mengi. Watu walimcheka kizee Nuhu wakisema, "anasema maji yataanguka toka juu na anajenga boti kubwa". Wakati huu mvua ilikuwa haijawahi kunyesha kwa kuwa mimea ilistawi kwa umande. Kwa kumcheka Nuhu walimcheka Mungu pia, kwa sababu Nuhu alikuwa mjumbe tu aliyefuata maelekezo ya Bwana. Watu wakikucheka unapomfuata Mungu, mkumbuke Nuhu. Baada ya kukamilisha ujenzi wa Safina, Mungu akamwambia Nuhu kwamba baada ya siku saba, ataleta mvua, nayo itanyesha siku 40 usiku na mchana, na kila chenye uhai kitakufa.

Nuhu alikuwa na miaka 600 alipoingia kwenye safina, yeyé na mkewe pamoja na watoto wake wa kiume watatu na wake zao, jumla watu nane tu. Wakamwana hawa walijitoa kabisa, maana wazazi wao waliachwa! Walipoona wanyama wawili wawili, au saba saba wakiingia kwenye safina, bila shaka walishtuka kidogo, lakini

wakaendelea na maisha yao. Nafikiri ni dhambi, kuridhika na kiburi vilivyowapa upofu. Walimcheka Nuhu kwa kukaa kwenye safina isiyoelea maana ilikuwa nchi kavu. Mvua ikaanza kunyesha na dhoruba kali. Watu walikimbia na kumsihi Nuhu afungue mlango. Nuhu alijaribu na kushindwa, akawaambia "Mungu Ndiye amefunga mlango". Pengine walipanda miti mirefu, lakini maji yaliendelea kujaa na kufunika miti na milima yote. Viumbe vyote viliangamia, kila kitu chenye pumzi, kikafa. Takribani gharika ilikuwa mwaka wa 2348 KK, nayo ilibadilisha sura ya dunia na kupunguza uzuri wake.

Kuna kipengele kingine cha kisa hiki hapa ambacho ni muhimu sana. Mungu anatangaza kwamba "ataweka Agano Lake" na watu Wake. Agano la Mungu ni ahadi Yake ya uaminifu na wokovu Wake. Katikati ya dhoruba, Mungu alitayarisha safina yenye usalama. Yesu Ndiye kimbilio letu nyakati za dhoruba, safina yetu ya usalama, kimbilio letu nyakati za taabu. Habari njema ya ajabu iliyoje—- Agano la Mungu ni uhakikisho Wake la milele wa usalama wetu katika safina ya neema Yake. Mungu anapenda kutunza Agano Lake, hebu basi na tumkaribie na kutafuta kujua mapenzi Yake leo.

Mungu akamkumbuka Nuhu na familia yake kwenye safina, akavumisha upepo na kufanya maji yapungue. Vilele vya milima vikaanza kuonekana, Nuhu akafungua dirisha la safina na kumtoa kunguru, naye akatoka akaenda huku na kule. Kisha akamtoa njiwa naye hakupaona pa kutua, akarudi kwenye safina. Nuhu akamtuma njiwa tena baada ya siku saba; akaja na jani bichi la mzeituni kinywani. Nuhu akajua maji yamepungua, na baada ya siku saba alimtoa njiwa tena, naye hakurudi tena ndani ya safina. Mwaka ulipita wakiwa ndani ya safina na maji yalikauka na Nuhu akafungua safina. Mungu akamwambia Nuhu, atoke katika safina na wanyama alionao. Ilikuwa tukio la ajabu, kuona wanyama wakiruka au kukimbia wakitoka kwenye safina. Nuhu akamjengea Mungu madhabahu, na kutoa kafara ya shukurani kwa Bwana. Mungu akambariki Nuhu akaamuru tena "zaeni mkaongezeke mkaijaze nchi". Kabla ya gharika chakula alichopewa binadamu kilikuwa cha mimea tu (Mwanzo 1:29), lakini sasa kwa ajili ya upungufu aliruhusiwa ale wanyama ambao ni safi, ila alikatazwa kula damu na mafuta ya mnyama (Walawi 11). Siku hizi kwa ajili ya uchafuzi, imethibithishwa kwamba ni salama zaidi kula vyakula vya mimea, hivyo ni vyema kulima ili kula chakula bora ambacho tangu mwanzo Mungu alimpatia mwanadamu. Isaya 65 inaonesha kuwa katika nchi mpya, mwanakondoo na simba watacheza pamoja, hivyo wanyama na wanadamu wote watarudia ile lishe ya kwanza ambayo Mungu aliitoa, isiyoua viumbe wengine.

Baada ya baraka kwa Nuhu, Bwana akasema "Sitailaani nchi tena kwa gharika". Kweli ilikuwa huzuni kuangalia mahame na uharibifu wa nchi pale palipokuwa na majengo mazuri. Akasema "Ninauweka upinde wangu mbinguni nao utakuwa ishara ya Agano kati Yangu na nchi" maji hayatakuwa gharika tena. Ndipo Bwana akaleta upinde wa mvua wa rangi saba za kupendeza kwa mara ya kwanza ili kuwapatia matumaini.

Mwaka wa 1975, watalaamu wa elimu ya mambo ya kale, waligundua mabaki ya safina kukarabati, Uturuki! Hakika hii ni mojawapo ya vitu vinavyotuongezea imani yetu katika Maandiko kwamba ni ya kweli kabisa. Neno la Mungu linaposema kitu, tuamini, na kutii. Mungu hakumwacha Nuhu aangamie pamoja na watu wafisadi na wenye jeuri. Alimwambia Nuhu alichohitaji kufanya ili kuokolewa. Vivyo hivyo, tunajua kile kitakachoujia ulimwengu hivi karibuni, na tumeambiwa jinsi ya kujiandaa. Maandalizi haya pia yanajumuisha kuimarisha akili kwa Neno la Mungu na kuweza kuwa na mahali pa kulima na ikiwezekana tuhamie mashambani. Miji mingi mikubwa haitakuwa salama na itakuwa na maovu ya kutosha. Zaidi ya kujihami, twapaswa kuwaonya watu kile kitakachoujia ulimwengu. Yesu alisema kwamba kama vile zilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku za mwisho, basi, tuwe na hekima, tujiweke tayari ili tusipotee. Mwaliko wa Mungu kwa Nuhu ulikuwa 'Ingia ndani ya safina' huo ulikuwa mwaliko wa wokovu, usalama, na ukombozi. Ilikuwa ni ahadi ya utunzaji wake leo, kesho na hata milele. Ilimpa Nuhu tumaini katikati ya machafuko ya ulimwengu huu. Mwaliko wa Bwana unatupa matumaini nasi pia. Katika Safina ya usalama Wake tunapata wokovu, usalama na ukombozi. "Na huu ndio ujasiri nilio nao Kwake, ya kuwa, Nikiomba kitu chochote sawasawa na mapenzi Yake, atanisikia. Na kama nikijua kwamba ananisikia, nimwombapo chochote, najua kwamba ninazo zile haja nilizomwomba".

*Haiwezekani kabisa kukadiria nguvu ya ushawishi wa baba au mama anayesali. Anamkiri MUNGU katika njia zake zote. Anawachukua watoto wake mbele ya kiti cha neema na kuwakabidhi kwa Yesu, akiomba baraka Zake juu yao. Ushawishi wa maombi hayo ni "chemchemi ya uzima." kwa watoto hao. Maombi haya, yanayotolewa kwa imani, ni msaada na nguvu ya mama Mkristo. Kupuuza wajibu wa kuomba pamoja na watoto wetu ni kupoteza mojawapo ya baraka kuu zaidi zilizo karibu nasi, mojawapo ya silaha kuu katikati ya mashaka, masumbufu ya maisha, wasiwasi, na mizigo ya kazi yetu ya maisha.

---

Mvua ya Gharika ilinyesha kwa siku ngapi? Ndege wa pili aliyetumwa kuangalia nchi alikuwa yupi? Ni lini mwanadamu aliruhusiwa kula nyama? Ni nini maana ya upinde? Kwa nini Nuhu alitoa kafara? Kwa sentensi chache sema jinsi ambavyo umepata ndani ya Yesu safina ya usalama?

**SIKU YA 10**
**(January 10)**

# Mnara wa Babeli

**- *Mwanzo 9-11***

Watoto wa Nuhu walikuwa Shemu, Hamu na Yafethi. Hawa ndio walizaana na kujaza dunia nzima tuliyonayo. Nuhu akaanza kuwa mkulima, akapanda mizabibu, na kuanza kunywa divai. Akalewa na kuwa uchi katika hema yake, Hamu, baba ya Wakanaani alipomwona akiwa uchi, aliwaeleza ndugu zake. Shemu na Yafethi wakaenda kinyume nyume na wakamfunika baba yao nyuso zao zikielekea nyuma. Ulevi ulipomtoka Nuhu, akajua mwana wake mdogo alivyomtenda akasema "amelaaniwa…atakuwa mtumwa wa ndugu zake." Nuhu alifanya dhambi kulewa, tunaamini aliiungama. Neno la Mungu linasema 'walevi hawataingia mbinguni". Wapo watu siku hizi wanafikiri kutembea bila nguo ni jambo jema. La hilo si jambo jema. Ni kosa kutembea bila nguo, au nguo za aibu.



Baada ya gharika, Nuhu akaishi miaka 350 akafa. Watoto wake waliendelea kuzaana, na nchi yote ilikuwa na lugha moja. Takribani mwaka wa 2242 KK, watu wakasemezana wakiongozwa na Nimrodi mwindaji, kujenga mnara na kilele chake kifike mbinguni ili wasipate kutawanyika usoni pa nchi yote kama walivyoagizwa na Bwana. Pia walisema mnara huo utawasaidia endapo gharika nyingine itakuja, japo Bwana aliwambia ameweka ishara ya upinde kwamba hataangamiza tena dunia kwa maji, lakini wao hawakusikiliza. (Watu wote waliishi karibu na mito ya Tigrisi na Frati).

Bila shaka wasingalifika mbali. Wataalamu sasa wanasema kuwa jua lipo umbali wa kilomita milioni 150, mwezi umbali wa kilomita 280,000. Je, kweli wangefikaje mbinguni? Jua letu ni mojawapo ya nyota zilizo karibu, bali zingine ziko maili mabilioni na mabilioni, hata kwa Roketi zinazosafiri maili 20,000 kwa saa zitachukua miaka mamilioni kufika huko. Huu ulikuwa ni uasi, yaani, kutaka kushindana na maagizo ya Mungu. Bwana akashuka aone na Akasema, "Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja, na haya ndiyo

wanayoanza kuyafanya, wala sasa hawatazuiliwa neno walilokusudia kulifanya". Bwana akawafanya wasisikilizane maneno wao kwa wao. Mmoja akimtuma mwenzake shoka, analeta jembe, basi hasira zikawapanda na kukatokea machafuko ya kutoelewana. Bwana akawatawanya usoni pa nchi yote kwa njia hii, wakaacha kujenga ule mji/mnara. Hapo ndipo Bwana alipoleta lugha tofauti duniani. Ilikuwa masikitiko, watoto wakiachana, wanajaribu kuagana, lakini walijikuta wanatamka maneno ya ajabu ambayo wenzao hawakuyaelewa. Ukihesabu miaka, inaonekana Nuhu aliishi/aliona matukio mawili mazito, tukio la gharika, yeye na watoto wake wakasalimika, na tukio la mnara wa Babeli ambapo aliona 'wajukuu' zake wakileta uasi mwingine. Pengine aliwaambia ila hawakusikia. Ni kweli "Mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake" Mwanzo 6:11. Ni neema ya Mungu tu inayotusaidia kuepuka uovu. Mpendwa msomaji, tusitumaini 'uzuri wetu.' Ni lazima tukubali Mungu atupatie uzuri Wake na kutuvika "kanzu ya haki yake" ili tuweze kupona. Kizazi cha Shemu kilipoendelea miaka mingi, alizaliwa Nahori, Naye Nahori akamzaa Tera aliyeishi Harani. Naye alizaa wana watatu ambao ni Abramu, Nahori na Harani. Mungu aliangalia akaona huyu anamwabudu katika kweli kama Nuhu. Abramu akajitwalia mke aitwaye Sarai ambaye alikuwa dada yake wa kambo. Sarai hakujaliwa kupata mtoto, alikuwa tasa. Tera akamchukua kijana wake Abramu, na mke wake Sarai, na mjukuu wake Lutu kwa Nahori ambaye alifariki. Akasafiri kutoka Uru wa Wakaldayo kwenda Kanaani. Walipofika Harani, Tera alikufa na kuzikwa akiwa na miaka 205.

Bwana akamjia Abramu akiwa hapo na kumwambia atoke kwenye nchi yake, alipoishi na jamaa zake aende katika nchi atakayomwonesha. "Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa na kukubariki, na kulikuza jina lako, nawe uwe baraka, Nami nitawabariki wakubarikio naye akulaaniye Nitamlaani na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa". Takribani miaka 1922 KK Abramu akamtii Mungu kama alivyoamuru, maana alijifunza kuijua sauti yake, akamchukua mkewe Sarai, Lutu mpwa wake, na vitu vyake. Abramu alikuwa na miaka 75 alipotoka Harani, akasafiri mpaka Shekemu. Hapa palikuwa na umbali wa km 1500, bila gari bali punda au ngamia. Wakanaani waliishi pale na Bwana akamwambia Abramu kuwa atampatia nchi ile, na uzao wake. Abramu akamjengea madhabahu Bwana aliyemtokea, na kuliita Jina la Bwana. Naye akaendelea kusafiri.

Kulikuwa na njaa katika nchi na hivyo Abrahamu akasafiri mpaka Misri, akae huko, maana kuna unyweshaji mazao kutokana na mto Nile. Wayahudi, Wakristo na Waislamu wanamchukulia Abrahamu kama baba wa imani zao. Mungu ana mipango kwako leo kama ilivyokuwa kwa Abramu! Kwa maana sisi tu taifa takatifu kwa BWANA, Mungu wetu; BWANA Mungu wetu, ametuchagua kuwa watu Wake, zaidi ya mataifa yote walioko juu ya uso wa nchi (Kumbukumbu 7:6). Maneno haya yalisemwa na Kristo kwenye nguzo ya wingu jangwani, na Musa alipewa kwa ajili ya wateule wa Mungu. Bwana hajauacha ulimwengu bila ushuhuda. Ana watu Wake watiifu hata leo kama wakati wa Abrahamu na Musa, waliochaguliwa Naye. Hao hawaufanyi ulimwengu huu kuwa makao yao, lakini wako hapa kushuhudia kwa ajili ya Mungu, na maadamu rehema Yake inadumu, ushuhuda ulio hai utatolewa na wajumbe hawa waaminifu wa Bwana, Je, nawe ungependa kujiandikisha leo kwenye jeshi hili kubwa?

*Maombi ya akina baba na mama Wakristo hayapuuzwi na Baba wa wote, Yeye aliyemtuma Mwanawe duniani ili akomboe watu kwa ajili Yake. Hatayakataa maombi yako na kukuacha wewe na wako kwenye makombora ya Shetani katika siku ile kuu ya pambano la mwisho. Ni juu yako kufanya kazi kwa usahili na uaminifu, Naye MUNGU ataimarisha kazi ya mikono yako.

---

Kwa nini Hamu alilaaniwa? Kwa nini kutumia pombe ni dhambi? Babeli ina maana gani? Ni ahadi gani Mungu alimpatia Abramu wakati alipomtokea? Dini tatu kubwa zinadai kuwa Abramu ni baba wa imani zao, ni zipi hizo? Je, mbinguni kutakuwa na lugha ngapi? Je, uko tayari kuhama kama Ibrahimu?

**SIKU YA 11**
**(Januari 11)**

# Abramu - Baba wa Wenye Imani

**- Mwanzo 13-14**

Abramu aliishi miaka 100 hivi baada ya Gharika. Watu walitawanyika kwenda mahali pengi. Abramu aliishi Uru, na wengine Afrika, India, Siberia, China na Ulaya. Watu walifanya kazi mbali mbali, nyumba nyingi za makumbusho zina vifaa walivyotumia wahunzi, vito au meli.

Mungu aliona kuwa kabla dunia haijaingia katika uovu mwingine mkubwa, amtafute mtu wa kutunza Kweli Yake, mtu atakayempenda na kuwa mtiifu Kwake, na kutiisha watoto wake kutunza Sheria za Mungu. Abramu hakuwa na kazi ndogo kwa kuwa ndugu na jamaa zake waliabudu miungu migeni, akiwemo na baba yake. Mungu alimtazama Abramu na kuona kwamba "Huyu ni kijana anayefurahisha moyo Wangu". Hata leo Mungu anaangalia wasichana na wavulana ambao hawatamwaibisha. Mungu anawaambia siri Zake na yale yatakayotokea katika historia ya dunia ya sasa na siku za mwisho jinsi atakavyookoa watu Wake. Mungu alimtokea Abramu kupitia ndoto na njozi. Abramu akawa baraka kwa binadamu. Enzi hizo hazikuwa na usafiri wa kisasa, na watu wa jamaa moja waliishi pamoja wakisaidiana. Ilikuwa vigumu kujiondokea tu, bila kujua unaenda wapi. Bila shaka majirani walimwuliza, na hata wengine kucheka "hivi unajiendea tu, bila kujua unakokwenda?" Lakini Abramu alimtii Mungu. Hivyo ndiyo tunavyopaswa kufanya leo. imetupasa tumtii Mungu anapotuambia jambo na kuzitunza Amri Zake.

Wakiwa Misri, Abramu alimwambia mke wake Sarai kwamba, kwa vile ni mzuri wa uso, "Wamisri watakapokuona … wataniua mimi na watakuacha hai, tafadhali useme wewe u ndugu yangu, iwe heri … na nafsi yangu iishi kwa ajili yako". Huu ulikuwa nusu ukweli na nusu uongo, kwani alikuwa mke wake, japo kuna ukweli kwamba Sarai alikuwa mdogo wake, wa baba mmoja ila mama tofauti. Alikosa imani, na kujilinda, na kusahau kwamba Mungu Ndiye atulindaye. Alipofika Misri, Farao aliona kwamba Sarai ni mzuri sana, na akamchukua nyumbani kwake, na kumtendea Abramu mema kwa ajili yake. Bwana akampiga Farao na nyumba yake kwa mapigo makuu kwa ajili ya Sarai, ndipo Farao alimwita Abramu na kumwambia "umenitendeaje? Mbona hukuniambia ya kuwa huyo ni mkeo?" Ulisema ni dada yako mdogo! Akamwamuru Abramu amchukue mke wake na aende zake, akawaambia wafanyakazi wake wamsindikize Abramu na mkewe na kila kitu alichokuwa nacho, dhahabu, fedha, mifugo, mahema n.k. Abramu ndiye wa kwanza kuandikwa kama nabii katika Maandiko Matakatifu.

Abrahamu akaenda kusini mpaka Betheli. Ulikuwa msafara mkubwa wa watu wengi pengine hata elfu, mifugo na mali. Jeshi lake tu lilikuwa na watu 318. Akafanya madhabahu akatoa kafara na kuliita Jina la Bwana. "Alikuwa akiutuzamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga, ni Mungu" Waebrania 11:16. Lutu



mpwa wake alikuwa na makundi ya ng'ombe, kondoo na hema; na mali zao wote zilikuwa nyingi. Ukatokea ugomvi kati ya wachungaji wa wanyama wa Abramu na Lutu, katika nchi ya Kanaani. Abramu akamwambia Lutu kwamba si vyema uwepo ugomvi kati yao au wachungaji wao, kwani wao ni ndugu. Kama baba mdogo, alikuwa mpatanishi na mfano mzuri kwa Mungu. Akamwambia, "Je, nchi hii yote haiko mbele yako? Basi ujitenge nami, nakusihi, ukienda upande wa kushoto, nitakwenda upande wa kuume, ukienda upande wa kuume nitakwenda upande wa kushoto". Lutu akaona bonde la Yordani na kwamba lina maji, akajichagulia bonde hilo, wakatengana. Abramu akakaa Kanani na Lutu akakaa bonde la karibu na Sodoma, na akaendelea kusogea Sodoma mpaka akaishi katika mji ule.

Watu wa Sodoma walikuwa wabaya na wenye kufanya dhambi nyingi mno juu ya Bwana. Hii ni shida hata kwetu siku hizi, tunapenda kukaa mijini kwa ajili ya huduma nzuri kama shule, maji au barabara. Zaidi ya asilimia hamsini ya watu hukaa mijini. Miji mingi ina uovu ambao ni rahisi watoto kuingia. Inatubidi tuombe sana, maana Mungu anaipenda miji, na miji hii ina matumaini bado. Lutu japo alikuwa mtu wa haki, lakini aliingia pabaya. Pale inapowezekana nyumba za watu zikae mbali mbali, zisisongamane, watu wapate mahali pa kulima na kufanya shughuli kwa mikono yao. Tukiwa hatuna la kufanya mawazo maovu huja moyoni kirahisi. Wakati mwingine tunafanya maamuzi ya mahali pa kuishi, kazi, na wenzi wetu kwa macho yetu. Kinachoonekana kuwa sawa kwetu kinaweza kisiwe kizuri mbele za Mungu. Roho ya Ibrahimu ya kujishusha ilimletea zawadi bora zaidi. Aliambiwa aangalie kote na akapewa nchi yote. Hii ilijumuisha upande wa mashariki ambapo Lutu alikuwa ameenda. Mungu alikuwa akimpa hata nchi ambayo Lutu aliichagua. Kinachoonekana kuwa hasara kwetu tunapochagua njia ya Mungu ni faida kwetu mwishowe. Kile alichochagua Lutu kikawa msiba kwa familia yake. Baada ya kutengana na Lutu, Mungu akamwambia tena Abramu, "nchi hii nitakupa na uzao wako milele, na nitaufanya uzao wako kuwa kama mavumbi ya nchi … uzao wako hautahesabika". Kuwa na ubia na Mungu si hasara kamwe!

Abramu akakaa mialoni ya Mamre, akamjengea Bwana madhabahu. Ikawa wafalme wa nchi za jirani walipigana vita na hata kuingia Sodoma na Gomora na kumteka nyara Lutu na mali yake wakaenda zao. Mtu mmoja aliyeponyoka alimjulisha Abramu. Naye aliposikia nduguye yu mateka, alichukua jeshi lake la watu 318 ili kumkomboa Lutu. Kumbuka enzi hizo hakukuwa na polisi au ambaye angepigiwa simu. Alifanya shughuli hii usiku wa manane na Mungu akambariki, akawapiga adui na kuwafukuza na kumrudisha Lutu, watu wake, na mali zake zote. Mfalme wa Sodoma akamshukru Abramu kwa kumsaidia. Abramu akatoa zawadi kwa Melkizedeki mfalme wa Salemu kuhani wa Mungu Aliye juu sana. Akasema,

"Abramu na abarikiwe na Mungu Aliye juu sana, Muumba wa mbingu na nchi. Ahimidiwe Mungu Aliye juu sana, aliyewatia adui zako mikononi mwako". Abramu akampa fungu la kumi au zaka Mfalme huyu wa Salemu. Hakuwa na baba au mama, Naye alikuwa mfano wa Kristo. Hakuna kinachojulikana kuhusu kuzaliwa au kifo Chake kwa sababu hakuna rekodi Yake. Kristo Naye hana mwanzo wala mwisho. Nasi pia tujifunze kutoa zaka kwa uaminifu katika mapato yetu yaani fungu la kumi.

Mfalme wa Sodoma akamwambia Abramu achukue mali zote ila ampe raia wake aliowakomboa. Abramu akasema hatapokea vitu vya mfalme huyu, alisema "sitatwaa uzi wala gidamu ya kiatu, wala cho chote kilicho chako, usije ukasema, nimemtajirisha Abramu." Alipokea chakula tu walichokula vijana wake, na watu waliokwenda naye kufanya ukombozi naye akaacha wengine watwae sehemu zao. Roho hii isiyokuwa na uchoyo ni moja ya sifa ya Abramu kuwa baba ya wenye imani.

*Maombi ya Familia Ni Muhimu, Lakini Aina Nyingine za Maombi Zinahitajika Vilevile—Maombi ya Familia au ya hadhara pekee hayatoshi. Maombi ya siri ni muhimu sana; katika upweke nafsi inafunuliwa na kuanikwa wazi mbele ya jicho la MUNGU lichunguzalo, na kila nia inapekuliwa kwa karibu na kikamilifu. Maombi ya siri! Ni ya thamani sana! Nafsi inazungumza/inawasiliana na MUNGU! Maombi ya siri yanapaswa kusikilizwa na MUNGU tu anayesikia maombi. Hakuna sikio la udadisi litakalopokea mzigo wa maombi kama hayo.

---

Kwa nini Lutu alienda kuishi Sodoma? Abramu alikwenda na watu wangapi kumwokoa Lutu? Je, Mungu akikwambia uende usipojua, utaenda? Kwa nini Abramu alichaguliwa na Mungu? Kurudisha zaka kuna umuhimu gani? Ni mambo gani yalimfanya Abramu kustawi? Melkizedeki mfalme wa Salemu ni nani? Kwanini mfano wa Ibrahimu wa kutokuwa na kinyongo ni mzuri kwa kila muumini? Leo kuna watu ambao wamechukuliwa mateka na ulevi, mahusiano machafu, na marafiki wabaya, Je, unafanya nini kuwaokoa?

**SIKU YA 12**
**(Januari 12)**

# Kuzaliwa kwa Ishmaeli na Ahadi ya Kuzaliwa kwa Isaka

**- Mwanzo 15-17**

Mungu alimtokea tena Abramu katika njozi na kumwambia, "Mimi ni ngao yako na thawabu yako kubwa sana". Abramu akauliza "Ee BWANA Mungu, utanipa nini, nami naenda zangu hali sina mtoto atakayemiliki, nyumba yangu", isipokuwa mtumishi wake Eliezeri, mdameski. Mungu akamwambia Eliezeri siyo atakayemrithi, ila mtoto wake wa kuzaa. Akarudia kumwambia tena, "uzao wako utakuwa kama nyota, usioweza kuhesabika." Hata leo sidhani kama kuna mtoto anayeweza kuhesabu nyota! Wanasema usiku wa anga shwari watu wameweza kuhesabu mpaka nyota 5000. Ila kuna mabilioni ya nyota, na inazidi kugundulika kwamba nyota hizi ni sayari, na mianga au majua mengine. Abramu akamwamini BWANA; na kwa imani yake, BWANA akamhesabia haki na kumkumbusha kwamba Yeye ni Mungu aliyemtoa kutoka Uru wa Wakaldayo ili ampe nchi ile airithi. Mungu akamwambia atoe kafara ili kumtoa mashaka kwamba atairithi nchi, Abramu akatoa ndama, mbuzi, kondoo na hua na mwana njiwa, alipasua vipande viwili kila mnyama na kuweka nusu kushoto na nusu kulia. Moto ulipita kati ya vipande viwili na siku hiyo BWANA akafanya agano na Abramu na kuwapa wazao wake nchi ya Kanaani, kutoka mto wa Misri, mpaka mto wa Frati. Alimwambia pia kuwa uzao wake utakuwa utumwani kwa zaidi ya miaka 400. Jambo hili lilitokea, walikuwa Misri miaka 430 ila 400 ndiyo ilikuwa ya utumwa. Pande mbili zikafanya mapatano au Agano hapa. Mungu na Ibrahimu. Kama vile Ibrahimu alivyokesha na kuangalia tai wasile kafara, nasi tunahitaji kuwa na bidii sawa katika kukesha kwenye maombi ili kuhakikisha Shetani hafanyi uharibifu kwetu. Hapa ndipo tohara iliagizwa. Leo Tunatarajia kupitia tohara tofauti katika agano jipya la Mungu pamoja nasi leo: "Basi zitahirini govi za mioyo yenu, wala msiwe na shingo ngumu tena. Kwa kuwa BWANA, Mungu wenu, Ndiye Mungu wa miungu, na Bwana wa mabwana, Mungu mkuu, Mwenye kuogofya, asiyependelea mtu wala kupokea rushwa. Hufanya hukumu ya haki kwa yatima na mjane, Naye humpenda mgeni kwa kumpa chakula na mavazi; basi mpendeni mtu baki, kwa maana ninyi mlikuwa wageni katika nchi ya Misri; mcheni Bwana, Mungu wenu; mtamtumikia Yeye na kushikamana Naye na kuapa kwa Jina Lake, Yeye Ndiye sifa yako, na Yeye ndiye Mungu wako, aliyekutendea mambo haya makubwa na ya kutisha, uliyoyaona kwa macho yako" (Kum 10:16-21).

Sarai alipoona bado hajapata mtoto, alimchukua mjakazi wake Mmisri, aitwaye Hajiri na kumwambia Abramu amtwae ili apate uzao kwa yeye. Hapa Sarai alifuata kanuni za upagani, hili lilikuwa kosa la kutoamini. Mungu alitaka kumwinulia Abramu uzao kupitia Sarai na si mwingine. Akina mama wanapaswa kuangalia mashauri wanayokusudia kuyatoa. Wasitoe ushauri unaowakwaza waume zao. Na akina baba

wanapaswa kusimama imara kwa kutokubali ushauri mbaya, wakati wameshasikia sauti ya Mungu. Hajiri alikuwa msichana mdogo tu aliyewatumaini watu wazima hawa kama wazazi wake, ila wakapanga mikakati yao ambayo walifikiria inawafaa na kumwingiza dhambini naye, jambo hili ni makosa, nalo linatuonyesha kwamba kila mtu anahitaji msamaha wa Mungu, na hakuna aliye mkamilifu, ila tunapaswa kutubu mara tu tunapogundua. Japokuwa Abramu alifanya kosa hili, maana kila binadamu ana mapungufu yake, baadaye alijisahihisha na kumwacha Hajiri na mwelekeo wa maisha yake kwa jumla yalikuwa ni kumpenda sana Mungu, hata akaitwa 'rafiki wa Mungu'. Naurdia kusema kuwa 'ila ni jambo baya kwa watu wazima kumchukua msichana mdogo ambaye ni kama mtoto wao na kumfanyia jambo kama hili", ushauri huu haukuwa unaotoka kwa Mungu hakika!



Baada ya mjakazi kupata mimba, Sarai akaona kwamba Hajiri anamdharau, na kwamba yeye sasa anajiona ndiye mke na ndiye atamzalia Abramu mtoto wa ahadi. Sarai alimwambia Abramu tabia ya mjakazi, Abramu akasema kwamba yeye ndiye bosi, hivyo afanye anavyoona. Wanawake wale wawili, waligombana sana. Sarai akawa mkali na kumtesa Hajiri mpaka akakimbia. Alipofika jangwani akielekea Misri, katika kisima cha maji, malaika akamtokea na kumwuliza ni kwa nini anakimbia? Alipotoa sababu , malaika alimwambia, "rudi kwa Bibi yako na ukanyenyekee chini ya mikono yake". Akaambiwa kwamba uzao wake utazidishwa pia, na hautahesabika. Aliambiwa atazaa mwana na kumwita Ishmaeli, maana BWANA alisikia kilio chake na mateso yake. Hajiri aliita kile kisima "Mungu anionaye". Ishmaeli alizaliwa baba yake Abramu akiwa na miaka 86. Hakika twapaswa kuwa wavumilivu kwa ahadi za Mungu, ila mara nyingi tunajikwaa na kutokuwa na subira. Hebu tusitatue matatizo yetu kwa njia ambayo Mungu hapendi, hata ikiwa jamii inazikubali njia hizo. Kwa kufanya hivyo tunatengeneza matatizo makubwa kuliko yale tunayojaribu kutatua.

Ndoa za wake wengi ni kujiletea taabu, kwani zimesababisha huzuni nyingi kwa wengi. Pia kuna watu wenye hila zilizojificha, kwani wanakuwa na mke mmoja nyumbani, lakini wana mwanamke mwingine nje ya ndoa kama "kimada." na pia kuna mitara ya kuchukua mke na kumtaliki na kumchukua mwingine na kisha kumtaliki tena na kuendelea vile, hii ni mitara pia. Huzuni, dhambi na matatizo ya kudumu huendelea kwa njia hii. Hitimisho: Njia pekee ya kuwa na amani na furaha, kama ilivyo katika kila eneo la maisha, ni kufuata kielelezo kilichowekwa na Mungu na kuwa mwaminifu kabisa kwa nadhiri ya ndoa.

Mungu akamtokea tena Abramu akiwa na miaka 99 na akamwambia, "uende mbele Yangu ukawe mkamilifu". Ibrahimu alianguka na kusujudu. Mungu akamwambia kuwa atakuwa baba wa mataifa mengi. Bwana akambadilisha jina lake kuwa Ibrahimu na mke wake kuwa Sara. Akalifanya Agano Lake kuwa imara na kuwa la milele. Akamkumbusha ashike agano Lake na kila mtoto wa kiume atatahiriwa akifika siku ya nane. Pia alimwambia kuhusu tohara kuwa, "hii itakuwa ishara ya Agano Lake, na mtu asiyetahiriwa atatengwa." Alimwambia pia kuwa Sara atakuwa mama wa mataifa. Ibrahimu alicheka kicheko cha kutoamini na akajisemea, 'Je! Mtu wa miaka 100 aweza kuzaa kweli?" Mke wake Sara aliyekuwa na miaka 90 kwa desturi ya uzazi kwa wanawake alikuwa amekoma. Wanawake wengi hukoma uzazi wakifika miaka 50 hivi. Bwana alimwambia kuwa atambariki Ishameli kuwa taifa kubwa, ila Agano Lake ni kwa Isaka ambaye, "Sara angezaa majira kama yale mwaka uliofuata". Ibrahimu akatahiriwa na watu wote wa nyumbani mwake wa kiume akiwemo Ishmaeli aliyekuwa na miaka 13.

Ombi: BABA mpendwa tusaidie tujifunze na kulitumia somo hili kwa uzoefu wetu wenyewe, utujalie uwezo wa kuwa wavumilivu na kukusubiri Wewe daima, maana tunapokungojea tutabarikiwa zaidi, pia tutakuwa na amani ya akili na uwezo wa kukaa kwa umoja na wanaotuzunguka, asante BWANA kwa kusikia na kujibu ombi letu, katika Jina la Bwana wetu YESU Kristo tumeomba. Amina.

*Maombi na Ibada ni Muhimu kwa ajili ya Ukuaji wa Kiroho—Tafuta kila fursa ya kwenda mahali ambapo maombi yamezoeleka kufanywa (wana ratiba ya kufanya maombi). Wale ambao kweli wanatafuta ushirika na MUNGU wataonekana katika mkutano wa maombi, watakuwa waaminifu katika kufanya wajibu wao na kwa bidii na shauku kuvuna faida zote wanazoweza kuzipata. Wataboresha kila fursa ya kujiweka mahali ambapo wataweza kupokea miale ya nuru kutoka mbinguni.

---

Eliezeri alikuwa ni nani? Kwa nini Hajiri alikimbia? Ishmaeli ina maana gani? Tohara kwa watoto wa kiume ilikujaje? Kwa nini Mungu alibadilisha jina la Abramu? Ni nani aliitwa rafiki wa Mungu? Kwanini Mungu alimpa neema Hajiri, Sarai na Abramu? Je, unafikiri hata leo, Bwana anatupa nasi majina mapya?

**SIKU YA 13**
**(Januari 13)**

# Ibrahimu Azungumza na Mungu na Mvua ya Moto

**- *Mwanzo 18 na 19***



Siku moja mchana Ibrahimu alikuwa amekaa kwenye mlango wa hema lake katika Mialoni ya Mamre, akaona watu watatu waliokuwa wakielekea njia ile. Ibrahimu akapiga mbio kuwalaki. Alipowafikia alisujudu akisema, "BWANA wangu kama nimeona fadhili machoni pako nakuomba usinipite sasa mimi mtumwa Wako." Akawakaribisha maji ya kunawa miguu, chakula, na kuwaomba wapumzike kwake ili waburudike na kuendelea na safari. Wale wageni wakakubali. Hatujui Ibrahimu alijuaje kwamba Huyu ni BWANA na Malaika wawili. Hata hivyo tunaona mfano mzuri wa kutokuwa na choyo kwa wageni. Kwa sababu ya ukarimu, wengi wamekaribisha malaika bila kujua.

Wale wageni wakamwuliza Ibrahimu, "Yu wapi Sara mkeo?" Akawaambia, yupo hemani. Wakamwambia wakati huu mwaka ujao atapata mwana wa kiume. Sara aliposikia, kwa vile wote na mume wake walikuwa wazee, "akacheka", tunaweza kusema kicheko kilikuwa ni cha huzuni na kebehi. Akasema, "niwapo mkongwe, nitapata furaha na bwana wangu mzee?" BWANA akasema, "mbona Sara amecheka akisema mimi kweli nitazaa mwana nami ni mzee? Bwana akamkumbusha Sara, "Kuna neno gani lililo gumu kumshinda Bwana" Msomaji mtoto, isome ahadi hii na kuidai. Hakuna jambo gumu linalomshinda Mungu, ukiwa na shida au wazazi wako hawana chakula, mavazi, marafiki zako, au mambo ya shule, mkabidhi Mungu Naye atakushindia, hakuna gumu Kwake. Wewe piga magoti usali kwa imani, na umwambie shida yako. Sara akapata hofu, hakujua wageni wanajua yote na wamesikia, akakana akisema "sikucheka." Bwana akamwambia, "umecheka."

Wale wageni walielekeza nyuso zao Sodoma, wakaenda huku wakisindikizwa na Ibrahimu. BWANA akawaambia wale Malaika wawili, "Je, nimfiche Ibrahimu jambo ninalotaka kulifanya iwapo atakuwa taifa hodari na katika yeye mataifa yote ya dunia watabarikiwa. Kwa maana nimemjua kwamba atawamuru wanawe na nyumba yake baada yake waishike njia ya BWANA". Kweli Ibrahimu ni mfano kwa

akina baba, “wafundishe watoto wao kumtii Mungu na kuheshimu watu”. BWANA akamwambia Ibrahimu kwamba kilio cha Sodoma na Gomora kimezidi, na dhambi zao zimeongezeka sana, na kwamba anaelekea huko kuona ili ajue la kufanya. Ibrahimu alianza kumsihi BWANA asiharibu mji kama kuna watu 50 wenye haki, kisha alishuka hadi watu 45, akaendelea mpaka akafikia watu 10. BWANA akasema kuwa akiona wenye haki kumi katika Sodoma, hataharibu mji kwa ajili ya hao kumi. Basi BWANA akaenda Sodoma na malaika wawili na Ibrahimu akarudi kwake.

Akiwa ameketi penye lango la mji jioni, Lutu aliona watu wawili wakielekea Sodoma. Akaenda mbio ili kuwalaki. Inaonekana alijifunza ukarimu kwa wageni toka kwa baba yake mdogo Ibrahimu. Wale malaika walisema watakaa uwanjani usiku kucha. Lutu akawasihi sana nao wakakubali. Akawafanyia karamu ya mikate. Kabla ya kulala wenyeji wa Sodoma waliizunguka nyumba ya Lutu wakiamrisha awatoe wale ‘wageni wawili’ ili wawatende mabaya. Watu hawa walikuwa waovu na walikuwa na tabia ya dhambi ya “ushoga”. Lutu akaenda na kuwasihi kwamba huo ni uovu na kwamba ana binti wawili na yuko tayari kuwapa badala ya kuwafanyia ubaya wageni wake. Wale watu wakakataa katu, wakasema, Lutu ni mgeni na anajifanya kujua. Wakataka kumvamia Lutu, wakasonga karibu wavunje mlango.

Ndipo wale Malaika wakawapiga upofu wale watu hata wakachoka kwa kutafuta mlango. Kile Mungu alichokichukia jana, anakichukia leo pia, kwa maana anasema, “Mimi ni Bwana, sibadiliki.” Malaki 3:6. Kwa kuwa watu wamepitisha sheria zinazoruhusu wanaume kuoa wanaume, na wanawake kuoa wanawake, haina maana sheria Yake imebadilika. Basi wale malaika wakamwambia Lutu atoe mkewe, wanawe na mabinti zake mara moja, kwa sababu BWANA atauharibu mji ule. Lutu akawaambia wakweze, na wengine mpaka alfajiri, lakini alionekana kama anayecheza tu. Ilipofika alfajiri, malaika wakamhimiza Lutu atoke na mkewe na mabinti zao wawili. Naye akakawia kawia na malaika wakamshika mkono na kumtoa nje ya mji kwa kumhurumia, pengine wakiruka naye juu! Kama baba wa mji angepaswa kusikiliza haraka atoke ili awape moyo watu wa familia yake. Lutu akaambiwa ajiponye, na asitazame nyuma wala asisimame katika bonde ila aende mlimani. Lakini Lutu akaomba akimbilie Soari, mahali penye mji mdogo, japo malaika walitaka pia waangamize mji huo. Inaonekana bado alitaka kukaa mjini, japo alisema ni kwa ajili ya uchovu. Malaika alisema kwamba hataangamiza Sodoma mpaka Lutu aingie kwenye mji huo. Maskini Lutu, alichagua “Jiji” zuri kama mahali pa kuishi, kumbe alijiletea shida. Mali yake yote aliyoichuma na mahali alipopachagua palitetekea kwa moto siku ile. Hukumu za Mungu zimeanza kuonekana duniani kama viashiria vya siku ile kuu na ya kutisha, hebu tusiendelee kuishi katika dhambi, kama mwisho wa Sodoma na Gomora ulivyokuwa, ndivyo ulivyo uhakika wa kuangamizwa kwa ulimwengu huu siku za karibuni.

Mke wa Lutu aliangalia nyuma, pengine akikumbuka watoto wake au vitu vyake, akageuka na kuwa nguzo ya chumvi. Ndipo BWANA akaichoma Sodoma na Gomora na miji iliyokaribiana nayo, kwa kibereti kutoka mbinguni. Dhambi za Sodoma haikuwa ushoga tu, bali kiburi, kujivuna, ulafi, uvivu, machukizo na kutosaidia masikini Ezekieli 16:49, 50. Hata sasa tunaishi wakati wa mwisho, na

dunia itaangamizwa tena. Je! unajitayarisha kuwa na tabia ya kwenda mbinguni? Ibrahimu alishukuru mpwa wake kuokoka. Lutu alipona na mabinti zake wawili. Binti mkubwa alizaa mtoto ambaye alikuwa baba wa taifa la Moabu na mdogo alizaa mtoto ambaye alikuwa baba wa taifa la Amoni. Petro anatuambia kuwa Lutu alikuwa mtu wa Mungu na mwenye"haki", lakini maovu ya Sodoma yalimfanya atende dhambi. Hata nasi pia tuwe waangalifu wakati tunapochagua mahali pa kuishi, marafiki zetu, ili tusiingie uovuni.

*Maombi ya faragha, maombi ya Familia, maombi katika mikusanyiko ya hadhara kwa ajili ya kumuabudu MUNGU, haya yote ni ya muhimu. Na tunapaswa kuyaishi maombi yetu.Tunapaswa kushirikiana na Kristo katika kazi Yake.

---

Ni nani walikuja kuzungumza na Ibrahimu? Unajifunza nini kuhusu ukarimu wa Ibrahimu na Sara? Kwa nini BWANA alikuwa anaenda Sodoma na Gomora? Kwa nini Ibrahimu alisihi Sodoma isiangamizwe? Kwa nini Lutu alikimbilia Soari? Shibe na kutosaidia maskini vinawezaje kuwa dhambi? 2 Petro 2: 7,8 - unaelewaje hili fungu? Je, kuna Neno Mungu asiloliweza, nani alisema Maneno haya?


**SIKU YA 14**
**(Januari 14)**

# Kuzaliwa kwa Isaka

***- Mwanzo 20 na 21***

Ibrahimu alipita akisafiri nchi ya mfalme Abimeleki na hapa alimwambia tena Sara mke wake aseme yeye ni dada yake. Alisema hivi kwa vile Sara alikuwa mzuri wa uso, na mfalme angemwua na kumchukua Sara kuwa mke wake. Ibrahimu alipitia mtihani huu tena mara ya pili! Mungu alimjia Abimeleki kwenye ndoto na kumwambia "mwanamke huyu uliyemtwaa ni mke wa mtu". Abimeleki akaponea chupu chupu kifo na Mungu akamsamehe kwa vile hakujua ni mke wa mtu maana Ibrahimu alisema ni dada yake. Mfalme akaambiwa amrudishe na Ibrahimu ambaye ni nabii, atamwombea apate kuishi. Akaambiwa, usipomrudisha, utakufa wewe na watu wote ulio nao. Kweli wafalme wa zamani na hata watu mashuhuri au wenye mali siku hizi wana uovu na tamaa ya kumchukua kila mwanamke aonekaye ana uzuri wa uso! Abimeleki aliamka asubuhi na kuwaambia watumwa wake yaliyotokea nao wakaogopa sana! Akamwambia Ibrahimu umetutendea nini? hata ukaleta juu yangu na juu ya ufalme wangu dhambi kuu? Ibrahimu akasema alifanya kwa ajili ya hofu. Abimeleki akampa Ibrahimu nchi na fedha ya pole. Ibrahimu akamwomba Mungu, naye akamponya Abimeleki, mkewe na raia wake waliofungwa matumbo kwa utasa kwa ajili ya kumchukua Sara. Jambo hili lina fundisho kubwa, tunajifunza kutosema uongo na kutojichukulia wanawake au waume wa watu kinyume na mpango wa Mungu eti bora tunawaka tamaa. Je, nyakati fulani tunasutwa na wale wasioamini wanapokuwa waadilifu kuliko sisi wenyewe? Mungu anafanya kazi hata katika maisha ya "wapagani," ili kuwaokoa. Ni lazima tuwe waangalifu na kutowahukumu, kwa kuwa wao ni wenye thamani sana machoni pa Mungu, na pia wanaweza kuwa watimilifu zaidi kuliko sisi nyakati fulani.

Ibrahimu akahamia Gerari karibu na Wafilisiti na pale mke wake Sara akamzalia mtoto, naye wakamwita Isaka kama walivyoambiwa, maana yake 'kicheko'. Kicheko kile alichocheka cha kutokuamini kwamba atapata mwana. Ishmaeli hakumpenda Isaka na alianza kumkejeli au kumchokoza. Hii ilimfanya Sara akasirike na kumwambia Ibrahimu, "mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu Isaka". Ibrahimu hakupenda neno hili ila Mungu akamwambia "Sikiza sauti yake kwa maana katika Isaka uzao wako utaitwa". Ibrahimu aliamka asubuhi na kumpa Hajiri maji na mkate, akaondoka kurejea kwao. Ishmaeli alikuwa na miaka kama 14 hivi. Maji yaliisha akangoja afe yeyé na kijana, naye akaenda mbali asimwone Ishmaeli akifa. Ndipo mama mtu akapaza sauti akalia, Naye Mungu akasikia na kusema, "usiogope maana Mungu amesikia sauti yako". Alipofumbua macho, aliona kisima cha maji, akampa Ishmaili. Basi Bwana akamfanya Ishmaili kuwa taifa kubwa katika jangwa, naye akaoa Mmisri. Mpaka leo, watoto wa Ishmaili wanaishi katika jangwa la Uarabuni. Na watoto wa Isaka au Waisraeli wanaishi Israeli na mahali pengi dunia nzima. Kweli hakuna lisilowezekana kwa Mungu wetu.



Siyo kila kitu kiliwekwa kwenye Maandiko kinaweza kufahamika kwa ukamilifu, kwa hivyo tunalazimishwa kumwamini Mungu huyu wa ajabu ambaye ametoa habari nyingi, ila bado anaacha mengi hewani. Je, nina imani ya kutosha, na ujasiri wa kutosha kumwamini Mungu huyu anayedai kuwa Baba yangu? Hakika, tumepewa uwezo wa kufanya vile! Ikiwa tungekuwa na habari zote kwa undani kabisa, hatungehitaji kuwa na imani au ujasiri kwa Mungu, Kumbu Kumbu la Torati 29:29

*Katika mikutano yetu ya ibada au kujitoa wakfu kwa Mungu, sauti zetu zapasa zidhihirishe kwa maombi na kumsifu Mungu ibada yetu kwa Baba wa mbinguni, ili wote wajue kwamba tunamwabudu Mungu kwa urahisi/usahili na Kweli, na kwa uzuri wa utakatifu.

---


Ibrahimu alikuwa na umri gani alipomzaa mtoto wa ahadi? Kwa nini mtoto aliitwa Isaka? Kwa nini unafikiri Ishmaeli alimdhihaki Isaka? Kwa nini Mungu aliruhusu Ishmaeli aondoke? Nini kilitokea kwa Ishmaeli na Hajiri walipoenda zao jangwani? Je, wewe ni uzao wa Ibrahimu? Je, Uongo ni nini? (Kitabu cha Wazee na Manabii 309), Kwanini Mungu alimwambia Abramu amfanyie maombi Abimeleki?

**SIKU YA 15**
**(Januari 15)**

# Mtihani Mkubwa kwa Ibrahimu

***- Mwanzo 22-24***

Mungu alimpa Ibrahimu mtihani wakati Isaka alipofikia umri wa ujana. Mtihani wa utii. Mungu haruhusu binadamu kumtoa kafara binadamu mwingine bali huu ulikuwa mtihani kuona kama Ibrahimu alikuwa anampenda Mungu. Utii ni bora kuliko dhabihu na uasi ni kama uchawi alisema nabii Samweli. Bwana akamwambia Ibrahimu, "Umchukue mwana wako wa pekee, umpendaye Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria , ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima nitakaokwambia". Ibrahimu aliondoka alfajiri ili kutekeleza agizo hilo. Alichukua punda na vijana wawili wasaidizi pamoja na kuni kwa ajili ya kafara akaenda mahali alipoambiwa. Alikuwa mzee wa miaka 115 hivi. Akawaambia vijana wake wangojee chini ya mlima wakati yeyé na Isaka wanakwenda kuabudu. Alimchukua Isaka kule na kutayarisha kuni na moto, na kisu. Isaka akauliza, babangu "Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwanakondoo kwa sadaka ya kuteketezwa". Baba akajibu, "Mungu atajipatia mwana kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu". Baba alijenga madhabahu na kuweka tayari kuni kisha akamweka mwanawe juu ya madhabahu, juu ya zile kuni. Ibrahimu akanyosha mkono wake akakitwaa kisu



ili amchinje mwanawe, ndipo Malaika wa BWANA akamwita toka mbinguni akisema "Ibrahimu, Ibrahimu" naye akajibu "mimi hapa". Ndipo akaagizwa "usimnyoshee kijana mkono, wala usimtendee neno, kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee". Basi, Ibrahimu akainua macho yake na kumwona kondoo dume amenaswa pembe zake katika kichaka. Naye akaenda akamtwaa huyo kondoo na kumtoa sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe. Ibrahimu akapaita mahali pale Yehova Yire maana "katika mlima wa Bwana itapatikana". Mungu akajua kuwa Ibrahimu hakumzulia mwana wake wa pekee. Mungu akambariki tena kwa kumwambia atazidisha uzao wake uwe zaidi ya mchanga wa pwani, na mataifa watabarikiwa kwa kuwa alitii sauti ya Mungu. Hakika Ibrahimu alikuwa amepata mtihani, mtu mmoja alisema "Ikiwa hatubadilishwi kwa neema, basi hatuokolewi kwa neema".

Hakika, watoto wanaopenda kutii sauti ya Mungu wana baraka. Hata mtoto au kijana Isaka alitii, kwani angeweza kukimbia asifungwe kamba na baba yake ambaye alikuwa mzee, bali alitaka kumtii Mungu na mzazi wake pia. Utii ni somo la kwanza la muhimu kujifunza katika maisha yetu. Kisa cha Ibrahimu na Isaka kinatufundisha kuwa Mungu Ndiye mtoaji, na pia, kafara ya Mungu kumtoa Mwanawe pekee Kristo, kwa ajili ya dhambi zetu. Katika mlima huu wa Moria ndipo lilijengwa hekalu la Sulemani. Hatuwezi kujua mpango wa Mungu kwetu, ila jambo kubwa ni kumtumainia na kumtii, itakuwa bora kwetu mara zote kuwa watii. Mlima huu wa Moraya walioenda, watu wanasema pengine ndipo hekalu la Sulemani lilipojengwa.

Sara alifariki akiwa na miaka 127, ndiye mwanamke pekee umri wake upo kwenye Neno la Mungu. Ibrahimu akamlilia na kumwomboleza Sara. Akanunua pango la Makpela akamzika Sara, na hapo pakawa mahali ambapo familia ya Ibrahimu walizikia.

Baada ya kuwa na ukiwa, Isaka akamkumbuka mama yake. Alikuwa mtu mzima wa miaka 40, na Ibrahimu akamtuma mtumishi wake aliyeitwa Eliezeri, kilometa 1300 kule Harani au Iraki ya leo, kwa mpwa wake Labani ili amtafutie Isaka mke. Eliezeri akashika paja la Ibrahimu kama kiapo kwa ajili ya kumtafutia Isaka mke. Ibrahimu akasema, hata mke akikataa kuja huku "ujihadhari usimrudishe mwanangu huko". Nafikiri alijua kuwa ndugu zake walikuwa na miungu mingine na wala si Mungu wa mbinguni wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Hata hivyo alikuja Kanaani kwa ahadi ya Mungu "nitawapa uzao wako nchi hii". Eliezeri alichukua ngamia 10 na kufika Mesopotamia, akawapigisha magoti kwenye kisima ili wapate maji ya kunywa. Wanawake ndio waliokuwa wananywesha mifugo maji wakati huu na Eliezeri akamwomba Mungu ampatie ishara. Hii ndiyo sala ya kwanza iliyorekodiwa kwenye Biblia! Alisema, "BWANA Mungu, wa bwana wangu Ibrahimu, yule msichana nitakayemwambia tua mtungi wako, nakuomba ninywe maji, naye akisema unywe nami nitawanywesha na ngamia zako, basi huyu na awe ndiye uliyemchagulia mtumishi wako Isaka". Ni kazi nzito kumtafutia mtu mke. Vijana wengi siku hizi wanataka kutafuta wenyewe bila uchunguzi mzuri na wanaingia kwenye shida nyingi. Inasemekana nusu ya ndoa siku hizi huingia kwenye talaka. Basi kabla Eliezeri hajamaliza kuzungumza na Mungu, tazama akatokea

msichana anaitwa Rebeka ambaye ni jamaa wa Ibrahimu kwa Nahori. Hata wewe ukifika wakati wa kuwa na mwenzi wa maisha mkabidhi Mungu akuchagulie, kisha aongoze familia yako.

Hakika mtumishi mwema anakuwa kama mtoto wa familia! Katika safari hiyo ndefu angeweza kukimbia pamoja na watumwa na vito, lakini alikuwa mwaminifu kwa bwana wake. Alikwenda katika kazi aliyotumwa na kurudi tena, akitimiza kwa bidii na utii kile alichoamriwa. Majivuno yetu yasitufanye tusahau kuwa hata tukiwa na mali kila kitu ni cha Bwana na tutakuwa watumishi daima. Kwa hivyo siku moja, kama Eliezeri, thawabu yetu kuu itakuwa kutimiza utume wetu: kuonyesha tabia ya Bwana wetu na kuwa watiifu Kwake. Kabla hajamaliza kuomba, alijibiwa! "Niite, Nami nitakuitikia, Nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua?" Yeremia 33:3. Apataye mke apata kitu chema, Naye ajipatia kibali kwa BWANA. Mithali 18:22. Nyumba na mali ni urithi kutoka kwa baba, bali mke mwenye busara mtu hupewa na BWANA. Mithali 19:14. Ushauri wa wazee wenye uzoefu unapaswa kutafutwa katika suala la ndoa; ikiwa wakati wowote Biblia ilihitajiwa kuwa mshauri, ndiyo wakati huu! Ikiwa mwongozo wowote wa Bwana unaweza kutafutwa katika sala, ni kabla ya kuchukua hatua inayounganisha watu pamoja kwa ndoa! Njia moja ya kuhakikisha kwamba watoto wetu watachagua Wakristo wazuri kuwa wenzi wa ndoa ni wao wenyewe kuwa Wakristo wazuri.

*Jitayarishe kwa umilele kwa ari na bidii ambayo bado hujawahi kuoionyesha maishani mwako mwote. Ielimishe akili yako kupenda Biblia, kupenda mkutano wa maombi, kupenda saa ya kutafakari, na zaidi ya yote, saa ambayo nafsi inawasiliana na MUNGU. Kuwa na mawazo ya kimbingu ikiwa siku moja utaungana na kwaya ya mbinguni katika majumba ya juu.

---

Mungu alimpa Ibrahimu mtihani gani? Mungu alifanya nini kumsimamisha Ibrahimu asimchinje Isaka? Kwa nini Ibrahimu hakutaka Isaka aoe msichana yo yote? Kwa nini Eliezeri aliomba? Je, ni vizuri kuoa/kuolewa na mtu yoyote? Kwa nini?

**SIKU YA 16**
**(Januari 16)**

# Mke kwa Ajili ya Isaka

**- Mwanzo 24**

Eliezeri akapiga mbio kumlaki Rebeka, naye alikuwa msichana mwenye uso wa kupendeza. Rebeka alikuwa mjukuu wa kaka ya Ibrahimu Nahori. Eliezeri Akamwomba atue mtungi wake ampe maji ya kunywa, ndipo Rebeka akasema "unywe bwana wangu" akatua mtungi na kumpa maji. Alipokwisha kumnywesha maji akasema, atawapa ngamia zake maji. Ngamia mmoja, hunywa lita 30 za maji hivi. Huyu alikuwa msichana hodari, mwenye ukarimu na adabu kwa watu wazima. Rebeka alisomba mamia ya lita, bila kujua baraka zinazomngoja. Eliezeri alianza kujiuliza moyoni kama ndiyo huyu Mungu amempangia Isaka kuoa. Alimpa zawadi ya pete ya dhahabu na vikuku, kisha akamwuliza yeye ni binti wa nani? Alipojieleza aligundua kwamba ana ujamaa na Ibrahimu. Alimwomba kama kuna nafasi ya kulala kwao. Rebeka alimkaribisha kwao, akisema wana malisho ya mifugo.

Eliezeri alimshukuru Mungu kwa fadhila zake kufanikisha safari yake. Rebeka aliendा kumwambia kaka yake Labani, nao wakamkaribisha kwao. Wakamtunzia mifugo yake mahali pazuri. Aliandaliwa chakula lakini hakula mpaka aliposema haja yake. Alijieleza kuwa yeye ni mtumishi wa Ibrahimu na ametumwa kumtafutia mke, mtoto wa Ibrahimu aitwaye Isaka. Aliwaambia kuwa Mungu amembariki Ibrahimu, na angependa mtoto wake aoe kwao alikotoka. Akawaeleza safari yake na maombi yake yalivyokuwa. Ndipo kaka yake Rebeka na baba yake wakagundua kwamba "neno hili limetoka kwa Bwana". Wakakubali Eliezeri amchukue Rebeka kuwa mke wa Isaka. Eliezeri akalipa mahari kwa wazazi wa Rebeka. Wakala pamoja na kesho yake, Eliezeri aliaga ili kuondoka. Ndugu zake Rebeka wakasema kwamba akae siku kumi, lakini akasihi wasimcheleweshe maana BWANA ameweka kila kitu wazi. Basi walimwita Rebeka naye akakubali kwenda kuwa mke wa Isaka. Wakambariki "ndugu yetu na uwe wewe mama wa kumi elfu, mara elfu nyingi." Rebeka akaondoka na vijakazi wake, na wote wakapanda ngamia wakimfuata Eliezeri. Basi Isaka aliwaona alipokuwa akitoka kutafakari kondeni wakati wa jioni. Rebeka alishuka toka juu ya ngamia na kutwaa shela akajifunika. Eliezeri akamwambia Isaka yote yaliyotokea na Isaka akamwoa Rebeka na akampenda. Isaka akafarijika kwa kifo cha mama yake.

Ndoa ni mpango wa Mungu, na ni vyema pande zote kuzungumza, na si kwenda kuishi pamoja bila mipango ya kufunga ndoa. Tuombee ili tufuate mipango ya Mungu.

Hili ni fundisho kwa wasichana na hata wavulana wengi. Mara zingine baraka zetu zinakuja kwa njia ya ajabu kama Rebeka. Alikuwa ameshawahi kusikia kuhusu Abramu, na jinsi alivyo mtu wa imani na utajiri kuliko watu wengi, bali kwamba angeolewa na kijana wake, hakuwahi kulifikiria. Wema hauozi, sasa alikuwa

amepata bahati ya kuolewa mahali pazuri, na mume mwema. Je, ingekuwaje kama angeliamka na kuanza kununa, kuleta ukaidi au kuzira akiambiwa kufanya shughuli fulani? Sasa ni mmoja wa wanawake wanaosimuliwa katika historia ya dunia. Biblia ina wanawake takribani kama 182 tu kati ya wanaume 1182 hivi na Rebeka ni mmoja wapo, kwa ajili ya tendo lake moja jema! Alizaa mtoto aitwaye Yakobo (Israeli) ambaye jina lake linazungumzwa ndani ya Biblia kuliko la mtu mwingine (mbali na Kristo).

Inaonekana Isaka alikuwa mtu mwenye upendo, na asiyependa ugomvi japo alikuwa tajiri. Alichimba visima mara kadhaa na watu wakasema ni vyao katika nchi ya Wafilisti. Alipoona wanataka ugomvi, alienda kwingine na kuchimba kingine. Pia alimwita Ishmaeli wamlilie baba yao bila kinyongo. Kweli njia nzuri ya kushinda ubaya ni wema. Mwishowe alichimba kisima cha Beersheba, hicho ndicho hawakuja kuleta ugomvi nacho. Mungu alimtokea Isaka pia na kumbariki "Nitazidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, nami nitawapa uzao wako nchi hizi zote, na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watabarikiwa. Kwa sababu Ibrahimu alisikia sauti Yangu "ameyahifadhi Maagizo Yangu, Amri Zangu, hukumu Zangu, na Sheria Zangu". Wazazi wanaomtii Mungu wanabariki watoto wao sana, bali wale waovu wanalaani watoto wao.

Baada ya kifo cha Sara, Ibrahimu alioa mke mwingine naye aliitwa Ketura ambaye alimzalia wana sita. Isaka ndiye aliyekuwa mrithi wa kwanza kwa Ibrahimu. Ibrahimu aliishi miaka 175, akafa katika uzee mwema. Isaka na Ishmaeli na jamaa zake wakaja kumwomboleza. Akazikwa penye pango la Makpela. Ishmaeli aliishi miaka 137 naye akafa akiwa baba wa taifa kubwa.

Mazungumzo kati ya watu wa nchi na Ibrahimu ni ya kuvutia wakati wa kununua kipande cha kumzika mke wake. Walimwita "mkuu wa Mungu," (Prince of GOD) hakika walimheshimu kama mtumishi wa Mungu. Mbali na kumpokea Abrahamu vizuri, pia walitoa shamba aliloomba bila gharama yoyote. Hata hivyo, Abrahamu alijitolea kulipia shamba hilo kwa unyenyekevu. Kifo siyo mwisho wetu. Popote tunapozikwa hata kama majivu yetu yametawanyika, huo sio mwisho wetu. Tuna uhakikisho wa ufufuo wenye baraka wakati Yesu atakaporudi katika utukufu. ( 1 Wathesalonike 4:13-17 ) Tutapata fursa ya kukutana na Abrahamu, Sara, na watu wengine wengi wanaotajwa katika Biblia ambao wameokolewa kwa neema ya Mungu. Hakuna haja ya kutumia pesa nyingi kwenye kaburi Huko sio mwisho wetu. Mbingu na dunia iliyofanywa upya itakuwa makao yetu! Na bora zaidi, Mungu Mwenyewe atakuwa pamoja nasi na kuwa Mungu wetu, na atalifuta kila chozi katika macho yetu. Hakutakuwa na kifo tena, wala huzuni, wala kilio, na maumivu hayatakuwapo tena! "Nawaambieni kweli, wakati unakuja, na sasa umekuja ambapo wafu wataisikia sauti ya Mwana wa Mungu na wale wanaoisikia wataishi." "Kwa maana Mungu huyu Ndiye Bwana wetu hata milele na milele, na atakuwa kiongozi wetu hata kufa." "Mauti yatakuwa yamemezwa milele. Kisha Bwana Mungu atafuta machozi katika nyuso zote."

Huenda Abrahamu alifarijiwa na jambo hili kwa maana Biblia inasema juu yake na mashujaa wengine wa imani, "hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea

zile ahadi; walikuwa wageni na wasafiri juu ya nchi (Waebrania 11:13) Wazo hili na liendelee kuwafariji na kuwategemeza wajane na yatima wote kati yetu kwani hivi karibuni, "Mungu atafuta chozi yote katika macho yao" (Ufu. 21:4). Haleluya!

*Wakati Roho wa MUNGU atakapofanya kazi juu ya moyo, akilisafisha hekalu la nafsi na unajisi/uchafu wake wa mambo ya kidunia na kupenda anasa, wote wataonekana katika mkutano wa maombi, wakiwa waaminifu kufanya wajibu wao na kwa dhati, ari, jitihada na shauku ya kuvuna faida zote wanazoweza kupata. Mfanyakazi mwaminifu kwa Bwana ataboresha kila fursa ya kujiweka moja kwa moja chini ya miale ya nuru kutoka katika kiti cha enzi cha MUNGU, na nuru hii itaakisiwa juu ya wengine.

---

Kwa nini Rebeka alikuwa tayari kwenda na Eliezeri? Kaka ya Rebeka aliitwa nani? Ketura ni nani? Je, wema wa mtoto pia waweza kumbariki mzazi? Kwa jinsi gani? Ibrahimu aliishi miaka mingapi? Rebeka alionesha mfano gani mzuri kwa wasichana wa leo? Je, wazazi na ndugu za Rebeka walisemaje wakati Eliezeri alipowaambia jambo alilolifuata? Isaka anatupatia mfano gani wa kutunza amani na marafiki na jirani zetu?

**SIKU YA 17**
**(Januari 17)**

# Ugomvi wa Mapacha na Uzaliwa wa Kwanza

**- Mwanzo 25**

Isaka alimwomba Mungu kwa ajili ya mke wake. Rebeka alikuwa tasa, bila mtoto, na Bwana akamwitikia na akachukua mimba. Alikuwa na watoto mapacha tumboni na wakashindana, akakata tamaa na kusema " ikiwa hivi kuishi kwanifaa nini?" Alipomwuliza Mungu, akaambiwa kuwa "mataifa mawili yako tumboni mwako, na kabila mbili za watu watafarakana tangu tumboni mwako, kabila moja litakuwa hodari kuliko la pili, na mkubwa atamtumikia mdogo". Saa ya kuzaa ilipofika, pacha wa kwanza alitoka, naye alikuwa mwekundu, na hivyo akaitwa Esau au Edomu (nyekundu). Ndugu yake alitoka akimshika Esau kisigino, akaitwa Yakobo. Isaka alikuwa na miaka 60 watoto walipozaliwa. Watoto wakakua. Esau alipenda kuwinda wanyama nyikani na Yakobo alikuwa mtulivu mwenye kukaa hemani. Isaka akampenda Esau kwa sababu alikula mawindo yake na Rebeka alimpenda Yakobo. Kupenda mtoto mmoja kuliko mwingine ni jambo baya kwa mzazi, kwani inafanya watoto wafarakane. Inavyoelekea, inawezekana kulikuwa na majiko mawili hapa, baba akila na Esau, na mama akipika na kula na Yakobo.



Siku moja Yakobo alipika supu ya dengu, Esau akaja kutoka nyikani akiwa amechoka na akiwa na njaa. Akamwomba Yakobo ampatie dengu nyekundu alizokuwa anapika, huku akidai kuwa alikuwa anazimia. Yakobo akamwambia kwa hila kuwa amuuzie haki ya uzaliwa wake wa kwanza ndipo atampatia dengu. Esau bila kufikiri akauza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa chakula kisicho na thamani huku akisema, "tazama mimi ni karibu kufa, itanifaa nini haki hii ya uzaliwa wa kwanza?" Basi Yakobo akamwambia Esau aape, naye akamwapia kumpa haki yake ya uzaliwa wa kwanza. Esau akachukua mkate na dengu akala, na kunywa na kisha akaondoka.

Hivi ndivyo Esau alivyoidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Akauza utajiri mkubwa kwa bakuli la chakula tu. Jambo hili lilimtokea Hawa, aliuza kila kitu kwaajili ya tunda, chakula ni kitu cha kuwekea tahadhari. Hivyo ndivyo siku hizi wengi wanavyofanya kujiuza au kujidhalilisha, kwa mambo madogo yanayopita. Tuchukulie wokovu wetu kwa makini sana, ili tusiuze uzaliwa wetu wa kwanza kama alivyofanya Esau.

Esau alioa wake wawili mmoja aliitwa Yudithi na Basemathi, Wahiti. Inaonekana wake hawa walikuwa na magomvi na wakaleta huzuni kwa Isaka na Rebeka. Baadaye Esau alioa mke wa tatu, binti wa Ishmaili baba yake mkubwa. Nafikiri Esau hakuoa watu wa imani, bali wenyeji wa pale alipoishi, na kuoa wake wawili ni njia rahisi ya kujiletea magomvi mengi kwa vile haiendani na mpango wa Mungu. Baba yake alitoa mfano mzuri wa kuwa na mke mmoja, ila yeye hakuufuata.

Kwa nini Isaka alichukua muda kupata watoto ila Ishamaili aliendelea kupata watoto? Kwa nini wenye haki wanateseka? Nalazimika kukukatisha tamaa, kwa sababu sina jibu. Hata hivyo, ikiwa wewe mtoto wa Mungu una tatizo ambalo wengine hawana, jua tu kwamba wewe si mtoto wa kwanza wa Mungu kuwa katika nafasi hii. Amini usiamini, andiko hili ni la kweli kabisa: "Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja katika kuwapatia mema wale wampendao, yaani, wale walioitwa kwa kusudi Lake" (Warumi 8:28). Ni mbinguni tu ndipo tutakapata Ukweli kamili wa kauli hii. Endelea kumwamini Mungu basi!

*Uwepo wa MUNGU Hufanya Nyakati za Maombi na Ibada ya Hadhara Kuwa jambo la wakfu au takatifu—Uchaji wa kweli kwa MUNGU huchochewa na hisia ya ukuu Wake usio na kikomo na utambuzi wa uwepo Wake. Kwa hisia hii ya Yule Asiyeonekana, moyo wa kila mtoto unapaswa kuvutiwa sana. Saa na mahali pa maombi na huduma za ibada ya hadhara mtoto anapaswa kufundishwa kuiona kuwa ni takatifu kwa sababu MUNGU Yuko pale. Na kadiri kicho kinavyoonyeshwa katika mtazamo na mwenendo, hisia inayoichochea itazidishwa.

---

Esau na Yakobo walitofautianaje? Kwa nini uzaliwa wa kwanza ulikuwa muhimu? Kwa nini Esau hakujali uzaliwa wa kwanza? Je, unatoa ushauri gani kwa wazazi wenye upendeleo kwa watoto? Je, tukitaka kuoa au kuolewa tutumie njia gani kupata mwenzi?

**SIKU YA 18**
**(Januari 18)**

# Yakobo Achukua Baraka za Esau

***- Mwanzo 27 na 28***



Isaka alipokuwa mzee na macho yake yamepofuka, alimwita Esau mwana wake mkubwa na kumwambia, "nimekuwa mzee wala sijui siku ya kufa kwangu". Akamwagiza achukue silaha zake za kuwinda aende nyikani kuwinda, na kumwandalia chakula kitamu vile apendavyo, kisha amletee ili ale na roho yake imbariki kabla hajafa. Rebeka alisikia maagizo haya. Kwa hila akamwambia Yakobo, kwamba amesikia baba yake akisema na Esau ili amletee mawindo, na kumfanyia chakula kitamu ili ale na kumbariki mbele za BWANA kabla hajafa. Rebeka akasema, "mwanangu sikiliza sauti yangu, kama ninavyokuagiza, enenda sasa kundini ukanitwalie wana-mbuzi wawili walio wema, nami nitawafanya chakula kitamu kwa baba yako, namna ile aipendayo. Kisha utampelekea baba yako, apate kula na akubariki kabla ya kufa kwake". Yakobo akamwambia mama yake, kwamba Esau ni mtu mwenye nywele nyingi za mwilini (malaika), baba yake anaweza kumpapasa na hivyo kuona anamdanganya. Akasisitiza kwamba atakuwa mdanganyifu na kujiletea laana na wala si baraka. Mama yake Yakobo akasema, "laana na iwe kwangu na si kwako, sikia sauti yangu tu na enenda ukaniletee wana mbuzi". Yakobo akafanya kama alivyoagizwa na mama yake akaandaa chakula

kitamu namna mume wake Isaka alivyopenda. Kisha Rebeka akatwaa mavazi ya Esau mwanawe mkubwa na kumvika mwanawe mdogo Yakobo. Kisha akachukua ngozi ya wanambuzi na kumvika mikononi na shingoni. Akampatia Yakobo kile chakula kitamu na mkate ili ampelekee baba yake. Yakobo akaenda kwa baba yake na kusema, "Babangu" baba akaitika, " mimi hapa u nani wewe Mwanangu?" naye akadanganya kwa kusema ni Esau, mzaliwa wa kwanza, na kuwa amefanya kama alivyomwambia.

Yakobo akamwambia baba yake aondoke akae ale mawindo ili roho yake imbariki. Isaka alishangaa kwamba imekuwaje mawindo ya siku ile Esau amepata mapema. Yakobo akadanganya kwamba Mungu wa Isaka amemfanikisha. Isaka akawa bado na shaka na akamwambia Yakobo aje karibu ili ampapase. Alipompapasa, alisema "sauti ni ya Yakobo, lakini mikono ni mikono ya Esau". Isaka hakugundua kwamba ni mikono ya Yakobo, yenye manyoya ya mbuzi. Basi akambariki, kisha akamwuliza tena "Wewe ndiwe kweli mwanangu Esau?" akajibu "ndimi". Akaomba aletewe karibu mawindo ili roho yake imbariki. Yakobo akamsogezea baba yake chakula karibu akala, na kunywa mzabibu. Baada ya kumaliza alimwita Yakobo na kumbusu, akakaribia na akasikia harufu ya mavazi yake, akambariki akisema, "harufu ya mwanangu ni kama harufu ya shamba alilolibariki BWANA. Mungu akupe umande wa mbingu, na manono ya nchi, na wingi wa nafaka na mvinyo. Mataifa na wakutumikie. Na makabila wakusujudie, uwe bwana wa ndugu zako, na wana wa mama yako wakusujudie. Atakayekulaani alaaniwe, na atakayekubariki abarikiwe."

Ikawa Yakobo alipokuwa amebarikiwa na babaye Isaka na kutoka mbele yake, Esau akaingia na mawindo yake akiwa amepika chakula kitamu. Akamwambia babaye akae na kula mawindo ili roho yake imbariki. Isaka alishtuka sana na kuuliza, "u nani wewe?" Ndipo Esau akasema, 'ni mwanao Esau, mzaliwa wako wa kwanza". Esau akatetemeka tetemeko kuu sana na akauliza, "Ni nani basi yule aliyetwaa mawindo akaniletea?" Maana aliisha kula na kumbariki Yakobo, hivyo baraka ilikuwa imeshaenda kwa huyo. Esau aliposikia hivyo aliangua kilio kikubwa, akajua kuwa mdogo wake "mlaghai", alikuwa amemfanyia hila. Esau akaendelea kulia na kumsihi baba yake kama ana hata punje ya baraka iliyobaki ili apewe. Isaka akajibu kwamba alikuwa amemfanya Yakobo kuwa bwana wake na kwamba ndugu zake wote watamtumikia. Isaka akamalizia kwa kusema, "Angalia penye manono ya nchi patakuwa makao yako, na penye umande wa mbingu unaotoka juu. Kwa upanga wako wewe utaishi, nawe utamtumikia nduguyo, na itakuwa utakapoponyoka utalivunja kongwa lake katika shingo yako". Esau akamchukia Yakobo kwa ajili ya ule mbaraka, na akawaza moyoni mwake kuwa baba yao atakapokufa atalipiza kisasi kwa kumwua ndugu yake, Yakobo. Rebeka alipopata habari hizi, alimwita Yakobo na kumwambia makusudi ya Esau kumwua. Akamshauri aondoke mara na kukimbilia kwa Labani kaka yake ili ghadhabu ya Esau ipite asahau ubaya aliotendewa. Rebeka akasema, "kwa nini nifiwe nanyi nyote wawili siku moja?" Kweli wazazi wanaweza kuleta chuki kwa watoto wao.

Hata leo wapo wazazi kama Rebeka wanaofanya wanandugu wachukiane na hata kuuana. Rebeka anaonyesha tabia mbili tofauti kabla na baada ya kuolewa.

Mtu angefikiri angekuwa mke na mama mcha Mungu mwema kulingana na tabia yake alipokutana na mtumishi wa Abrahamu! Kama mwanamke, hii ilinifanya kutafakari kuhusu sisi kama wanawake kutaka kuchukua madaraka na wakati mwingine tunaona kama tunajua vyema zaidi kuwasaidia watoto wetu kuliko hata Mungu. Hawa alifikiri hivi kuhusu tunda, Sara alifikiria hivi kusuhu Hajiri licha ya ahadi ya Mungu kwake, na Rebeka akamdanganya Isaka kwa sababu ya upendeleo na kutaka kuharakisha ahadi ya Mungu kwa Yakobo kuwa mzaliwa wa kwanza wa familia. Vitendo hivi vilisababisha athari ya tabia katika vizazi vyote. Japokuwa Yakobo alipata baraka aliyoitaka, madhara yake yalikuwa makubwa, kwa kuwa hakumuona tena mama yake wala baba yake, kaka yake alitaka kumuua, alidanganywa na mjomba wake na familia yake yote ikawa haifanyi kazi. Ni gharama kubwa kiasi gani tunayolipa tunapoenda kwenye njia zetu wenyewe. Udanganyifu unaharibu sana. Mtu anashangaa kwa nini Udanganyifu na uwongo unaendelea katika familia zetu leo! Tunapaswa kumtegemea Bwana kila wakati, na siyo uzuri wetu au matendo yetu! Biblia ni Bibliografia yenye Ukweli peke yake! Haina kumsifia mtu anayetenda dhambi au kumpaka mafuta kwa chupa ya mgongo. Kila binadamu humo alikuwa na mapungufu isipokuwa YESU tu, Nasi leo tuna mapungufu mengi, ila tukumbuke katika Warumi 5, wakati tungali wenye dhambi Masihi alikuja kwetu kama "Imanueli, Mungu pamoja nasi" (Mathayo 1:23). Ngazi ambayo Yakobo aliona inamwakilisha Yesu (Yohana 1:51), na uhusiano kati ya Mungu na wanadamu wenye hatia. Familia ya kibinadamu inaweza kuwa na upweke, hofu, na uchovu, lakini Mungu hajatupa kisogo. Hakika Yeye ni Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo-Mungu wa watu wote wanaohangaika na familia zenye matatizo. Tafadhali badilisha mioyo yetu Bwana Mungu nakusihi. Amina.

Siku zile mzaliwa wa kwanza alirithi mali maradufu. Jambo hili linaendelea mahali pengine na wasichana kwa kawaida hawana urithi, labda kule watakapoolewa.

Rebeka akamwambia Isaka kwamba anamtuma Yakobo kwenda Mesopotamia, kule alipotoka kupata mke kwa kaka yake Labani. Isaka akamwita Yakobo na kumbariki na kumwambia asitwae binti wa Kaanani bali aende kwa ndugu za mama yake ili ajitwalie mke. Akasema, "Mwenyezi Mungu akubariki, akuzidishe, na kukuongeza ili uwe mkutano wa makabila. Akupe mbaraka wa Ibrahimu, wewe na uzao wako, pamoja nawe, upate kuirithi nchi ya kusafiri kwako, nchi ambayo Mungu alimpatia Ibrahimu." Maskini, badala ya msafara kama ule wa Eliezeri alipokwenda kumtafutia mke baba yake, Yakobo alikwenda kama mkimbizi tu. Mungu alikuwa amesema 'mdogo atamtawala mkubwa', kwa hiyo Yakobo angeacha Mungu atimize mpango wake, badala ya yeye kuwa mlaghai.

Yakobo alikimbia hasira ya kaka yake, akatoka Beer-Sheba na kuelekea Harani. Alipokuwa anasafiri, alifika mahali fulani akalala hapo; alitwaa jiwe na kulitumia kama mto, akalala usingizi. Usiku akaota ndoto, na tazama aliona ngazi imesimamishwa juu ya nchi na ncha yake ilifika mbinguni. Akaona malaika wanapanda na kushuka juu yake. Ndoto hii ilionesha kuwa Mungu ameweka ngazi na Malaika ni wajumbe wanaounganisha mbingu na wanadamu. Akamwona BWANA amesimama juu ya ile ngazi, akisema "Tazama Mimi ni BWANA, Mungu wa Ibrahimu baba yako na Mungu wa Isaka, nchi hii uilalayo nitakupa wewe na

uzao wako, na uzao wako utakuwa kama mavumbi ya nchi, … jamaa zote za dunia watabarikiwa, na tazama Mimi nipo pamoja nawe, Nitakulinda kila uendako, Nami Nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana Sitakuacha, hata Nitakapokufanyia hayo Niliyokuambia." Kweli Mungu ni mwenye huruma, tukiomba msamaha na kuwa na toba ya Kweli kwa dhambi yoyote kubwa au ndogo, Anatusamehe na kutupatia matumaini. Yakobo alikuwa anakimbia kutokana na kosa la udanganyifu alioshirikiana na mama yake, lakini Mungu alimpenda na akaendelea kumwonesha upendo Wake. Yakobo alipoamka usingizini aliogopa sana, akasema, "kweli Bwana Yupo mahali hapa, wala mimi sikujua". Akaona ni mahali pa kutisha na akapaita "Betheli" maana yake nyumba ya Mungu. Asubuhi yake Yakobo alitwaa lile jiwe alilolalia na akalisimamisha. Akaweka nadhiri kwamba Mungu akiwa pamoja naye na kumlinda na kumpatia nguo na chakula katika njia anayoiendea, basi akirudi kwa amani nyumbani kwa baba yake, "ndipo Bwana atakuwa Mungu wangu" na "katika kila utakachonipa hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi (zaka)".

Kimsingi Yakobo alikuwa mbwa mwitu katika ngozi ya mbuzi. Kwa kufanya hivi alijipa hisia za Esau ila sauti ikabaki kuwa ya Yakobo. Je, haya si yaliyomo ulimwenguni leo? Watu wana hisia za kidini lakini sauti ni ya udanganyifu? Kujiita waumini lakini hukana mafundisho ya msingi ya Biblia. Paulo katika barua yake kwa Timotheo anarejelea kwa kusema ni kuwa na namna ya utauwa lakini tukikana nguvu zake. Ibilisi hajali kwamba tunaenda kanisani au kujiita Wakristo ilimradi ibada zetu ni za nje na tunazungumza kwa udanganyifu kwa ndugu. Anapenda kutushambulia kwenye udhaifu wetu. Hatujaachwa peke yetu. Malaika wa Mungu wanapanda ngazi na kushuka ili kutusaidia. Yakobo aliyedekeshwa akazaliwa upya baada ya mambo magumu aliyoyapitia. Naye Esau alidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Tunamwona akilia kwa huzuni kwamba hakupokea baraka zinazokuja kama haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Ila ukweli ni kuwa hakupendezwa na majukumu yanayohusiana na haki ya mzaliwa wa kwanza ila alitaka baraka tu. Hii ni kama mtu asiyependa kutenda mapenzi ya Mungu naye ni Mkristo, ila ataka tu kubarikiwa kiuchumi, kijamii, na kiafya tu. Kuikana nafsi yake na kujenga ufalme wa Mungu hakika sio lengo lake.

Mungu anatupa vichochoro vya giza vya mashujaa wa imani katika Biblia, ambao tuna hakika kuwa waliokolewa mwishowe, ili kutupa uhakikisho kwamba sisi pia, licha ya maisha yetu mabaya ya nyuma, tunaokolewa ikiwa tunatubu. Kwa kuwa tumesamehewa na Mungu dhambi zetu zilizopita, hebu tujisamehe wenyewe na tuache kujiuliza kama Mungu anatukubali. Yeye kamwe hamtupi yeyote anayekuja Kwake (Yohana 6:37)! Mungu ametupa nasi leo ngazi ifikayo Kwake, yaani kutoka duniani hadi mbinguni. Juu ya ngazi hii Yuko Mungu, anatutazama sisi tunaopanda, na tunapolegea hutuma msaada, tujiambie maneno yaliyojaa uchangamfu na matumaini maana mifano yote ya Biblia ni mafundisho yetu. Hakuna yeyote ambaye kwa ustahimilivu atapanda ngazi na kushindwa kupata mlango wa kuingia katika mji wa mbinguni.

Mamilioni leo wanauza haki yao ya uzaliwa wa kwanza kwaajili ya anasa za dunia. Afya imetolewa dhabihu, uwezo wa kiakili unadhoofika, na mbingu inapotea; na yote haya ni ajili ya starehe ya muda tu inayodhoofisha na kudhalilisha tabia.

Kama vile Esau alivyozinduka na kuona upumbavu wake wa kubadilishana haki yake kwa haraka haraka, alikuwa amechelewa sana kukomboa hasara yake, basi ndivyo itakavyokuwa katika siku ya Bwana kwa wale ambao wamebadilishana urithi wao wa mbinguni kwa ajili ya kujifurahisha kwa kitambo tu.

*Haijalishi ikiwa Maombi yatatolewa katika mkutano wa hadhara, kwenye madhabahu ya familia, au kwa siri, daima humweka mtu moja kwa moja mbele za MUNGU. Kwa maombi ya kudumu vijana wanaweza kupata kanuni zilizo thabiti/ imara sana kiasi kwamba majaribu yenye nguvu zaidi hayatawavuta kutoka katika uaminifu wao kwa MUNGU.


---

Kwa nini Rebeka alitaka Yakobo apate haki ya mzaliwa wa kwanza? Je, Rebeka na Yakobo walitenda haki? Kwa nini Isaka alikuwa na mashaka kwamba 'ni Esau kweli'? Kwa nini Esau alimchukia Yakobo? Kwa nini Yakobo alibarikiwa japo alikuwa mdanganyifu? Nini maana ya Betheli? Zaka ni nini?

**SIKU YA 19**
**(Januari 19)**

# Familia ya Yakobo

**- Mwanzo 29-31**



Yakobo alisafiri mwendo wa km 730 kwenda Harani. Mungu anatuhakikishia binadamu tunaposafiri na kumtumiani Yeye "Tazama Mimi Nipo pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari. Basi alipofika, alingoja karibu na kisima ambacho Eliezeri alimwona mama yake Rebeka. Alipokuwa akingoja aliona makundi matatu ya kondoo yakiwa yamelala, na jiwe kubwa likiwa limefunika kisima. Makundi yakikusanyika watu huviringisha jiwe na kunywesha mifugo yao. Yakobo akaanza kuzungumza nao akasema, "ndugu zangu watu wa wapi nyinyi?" Wakasema ni watu wa Harani. Akawauliza kama wanamjua Labani mjomba wake, wakasema wanamjua, na wakamwonesha binti yake Raheli aliyekuwa anakuja kunywesha kondoo. Yakobo alipomwona, alikwenda akaliviringisha jiwe na kumsaidia Raheli kuinywesha mifugo ya mjomba wake Labani. Akajitambulisha kwake na kumwambia kwamba yeye ni ndugu wa baba yake na mwana wa Rebeka. Labani aliposikia habari hizi, alikwenda na kumlaki Yakobo na kusema, "ndiwe kweli mfupa wangu na nyama yangu". Akakaa kwake kwa muda wa mwezi mmoja. Labani akamwambia ampe mshahara kwa vile anamsaidia kazi. Mzee Labani alikuwa na mabinti wawili, mkubwa aliitwa Lea na mdogo Raheli. Yakobo alimpenda Raheli na kusema, "Nitakutumikia miaka saba kwa kumpata Raheli binti yako mdogo". Labani alikubali. Miaka saba ilipopita, Labani alifanya karamu na ilipofika jioni alimtwaa Lea na kumpa Yakobo badala ya Raheli. Ilipofika asubuhi, Yakobo aligundua kuwa amepewa Lea. Ule ulaghai wa kudanganya aliomfanyia Esau, sasa alifanyiwa yeye. Yakobo alimkasirikia baba mkwe wake Labani lakini haikusaidia. Aliambiwa mkubwa huolewa kabla ya mdogo. Yeye alimpenda Raheli na kufikiri kwamba Lea hana uzuri wa sura. Labani alimwambia kuwa baada ya siku saba za arusi, atampa Raheli na Yakobo amtumikie miaka saba mingine kama mahari kwa ajili ya Raheli. Baba yake Yakobo alikuwa na mali nyingi, na angeweza kupata mahari kirahisi tu, lakini sasa alikuwa mkimbizi.

Hivyo Yakobo alijikuta anaoa wake wawili katika muda wa kama juma moja, akiwa na miaka 84 hivi. Lea alikuja na mjakazi wake Zilpa, na Raheli alikuja na mjakazi wake Bilha. Bwana akaona kwamba Lea hakupendwa akafungua tumbo lake naye akazaa, bali Raheli alikuwa hazai. Lea akazaa mvulana wa kwanza akamwita

Reubeni, wa pili akamwita Simeoni, wa tatu akamwita Lawi, na wa nne akamwita Yuda. Raheli alikasirika na kumwambia, Yakobo “Nipe wana la sivyo nitakufa”. Yakobo akakasirika na kusema, “mimi ni badala ya Mungu aliyekuzuilia uzao wa mimba”. Nyumba ikakosa amani. Raheli akampa Yakobo mjakazi wake Bilha ili awe mke wake. Bilha akamzalia mwana wa tano akamwita Dani, na Naftali wa sita. Lea naye akampa Yakobo mjakazi wake Zilpa, naye akazaa mwana wa saba, akamwita Gadi na wa nane Asheri. Ugomvi ukaendelea kati ya dada hawa wawili, huku Yakobo akimpendelea Raheli wazi wazi. Mungu akambariki tena Lea akazaa wana wawili, Isakari wa tisa na Zabloni wa kumi. Kisha akazaa binti akamwita jina lake Dina. Mungu akamkumbuka Raheli akamfungua tumbo akapata mimba na kumzaa mwana wa kumi na moja akamwita Yusufu, maana yake “Bwana aniongeze mwingine.” Na baadaye kabla hajafariki alimzaa Benyamini.

Yakobo alimtumikia Labani miaka mingine sita kwa ajili ya kujipatia mali. Jumla ikawa miaka 20. Kuoa wake wawili ni jambo baya na kuoa dada wawili ni mbaya zaidi. Dada hawa waliendelea kugombana. Baba yao na Yakobo ndio walikuwa na uwezo wa kuepusha ugomvi huu. Yakobo aliona Labani akimpunja mshahara wake na kuubadilisha kila mara. Labani aliona Mungu anambariki Yakobo, mali yake ilikuwa haba lakini iliongezeka sana wakati Yakobo anaisimamia. Labani alikuwa mtu mgumu japokuwa Yakobo sasa alihesabika kuwa wa mmoja watoto wake maana binti zake wawili walikuwa wameolewa na Yakobo.

Basi waliwekeana ahadi kwamba wanyama wote watakaozaliwa wenye ngozi ya rangi ya milia/marakaraka wawe wake na wa aina nyingine wawe wa Labani. Mungu akambariki Yakobo wanyama wake kama kondoo, punda, ngamia na hata wajakazi wakaongezeka. Labani na wana wake wakaanza kusema, “amechukua mali yote ya baba yetu, na kwa mali ya baba yetu amepata fahari hii yote”. Akaona kuwa wakwe zake hawakumtazama vyema tena. Bwana akamwambia Yakobo aondoke na kurudi kwa baba yake huko Beer-sheba naye atakuwa pamoja naye. Yakobo akatuma ujumbe kwa wake zake akawaambia, uso wa baba yenu “hanitazami vyema kama jana na juzi. Lakini Mungu wa baba yangu amekuwa pamoja nami. Nanyi mmejua ya kwamba kwa nguvu zangu zote nimemtumikia baba yenu. Na baba yenu amenidanganya, akanibadilishia mshahara wangu mara kumi. Lakini Mungu hakumwacha kunidhuru”. Basi Bwana akamwambia “ondoka, toka katika nchi hii urudi nchi uliyozaliwa.” Lea na Raheli wakakubaliana kuhusu baba yao, wakasema, “ametuuza, naye amekula fedha zetu kabisa”. Wakaona kwamba “Mali yote ambayo Mungu amemnyang’anya baba yetu, mali hiyo ndiyo yetu na ya wana wetu, wakasema “yote Mungu aliyokwambia uyafanye”. Wakaondoka bila kumuaga Labani, familia, au wafanyakazi wake. Akaenda na mifugo aliyopata kama mshahara wake. Raheli akaviiba vinyago vya baba yake aliyekuwa hayupo. Siku ya tatu Labani akaambiwa Yakobo amekimbia na akamfuata kwa siku saba. Mungu akamjia Labani katika ndoto na kumwambia, “Ujihadhari usimwambie Yakobo neno la heri wala shari”.

Alipofika alimwuliza Yakobo “Umefanya nini? Umenihadaa, ukawachukua binti zangu kama mateka waliotwaliwa kwa upanga, mbona umekimbia kwa siri”. Akasema alitaka aagane naye na binti zake kwa furaha, na nyimbo na ngoma na

kinubi na kuwabusu. Akamwambia Yakobo ametenda upumbavu na kwamba ana uwezo wa kumdhuru ila katika ndoto alionywa. Akaulizia miungu yake na Yakobo bila kujua akasema, "awaye yote utakayemwona kuwa nayo miungu yako yeye asiishi". Aliona kwamba hakuna katika mji wake anayeabudu miungu mingine, hakujua kuwa mke wake bado alikuwa na mapokeo hayo. Akamwambia Labani, "Naliogopa nikasema usije ukaninyang'anya binti zako kwa nguvu".

Hakika tupate faraja, na kuungama dhambi zetu, maana Yeye amesema "Ni Neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika, kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni, kwaajili ya kuwaokoa wenye dhambi. Kicho cha kweli kwa Mungu kinaongozwa na hisia ya ukuu Wake usio na kikomo na utambuzi wa uwepo Wake. Baada ya maombi Yakobo alijua anatembea na Bwana, yaani Mungu Yuko naye. Mungu alioonyesha upendo usio na masharti kwa Yakobo, Upendo huo ameuonyesha kwa kila mwanadamu. "Maana ni shida mtu kufa kwa ajili ya mwenye haki; lakini labda mtu angethubutu kufa kwa ajili ya mtu mwema. Bali Mungu aonyesha pendo Lake Yeye Mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi." Warumi 5:7-8. Sisi wenye dhambi tunapoona na kuthamini upendo huu, mioyo yetu inayeyuka na tunajitoa kwa Kristo kama Bwana na Mwokozi. Hivyo wema wa Mungu hutuongoza kwenye toba (Rum. 2:4).

Swali ni: Je, watu walio nje ya Kristo watauonaje upendo huu? Yapaswa wauone kupitia wanafunzi Wake. Hivyo ndivyo Yesu anamaanisha anapowaambia: "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni." Mathayo 5:16. Bwana Yesu, tafadhali ishi maisha Yako ndani yangu. Kwa Jina lile tukufu, Amina.

*Maombi ya Hadhara Hayapaswi Kuwa Marefu na makavukavu—Kama watoto wa Mfalme wa mbinguni, mnapaswa kujielimisha wenyewe kutoa ushuhuda kwa sauti iliyo wazi, inayotambulika, maneno yakitamkwa vizuri na kueleweka, na kwa namna ambayo mtu yeyote asiweze kuwa na hisia kwamba mnasitasita kuzungumza juu ya rehema za Bwana. Katika mkutano wa kijamii, sala inapaswa kutolewa ili wote waweze kujengwa, na wale wanaoshiriki katika zoezi hili wanapaswa kufuata mfano tuliopewa katika sala nzuri ya Bwana kwa ulimwengu.

---

Je, Yakobo alimwuliza Mungu kuhusu mke anayetaka kumwoa? Kwa nini Labani alimdanganya Yakobo? Kwa nini Yakobo aliamua kurudi nyumbani kwao? Unafikiri maisha ya dada wawili, yaani Lea na Raheli yalikuwaje kwenye ndoa? Je, unafikiri Yakobo na Labani waliaminiana? Kwa nini? Kwa nini Raheli aliiba vinyago? Taja majina 13 ya watoto wa Yakobo. Je, Yakobo alilipwaje ulaghai wake? Mungu alitoa mfano kwa Adamu wa mke mmoja, unafikiri kwanini watu hawaufuati mpango huu wa Mungu? Mungu aliona yote aliyofanya Labani, Je, hili linatupa faraja gani kwa Labani tunaokutana nao maishani mwetu leo? Unafikiri Yakobo ndiye aliyejisaidia mwenyewe kupata mifugo mingi kwa sayansi yake, au ni Mungu Ndiye alimbariki?

**SIKU YA 20**
**(Januari 20)**

# Mweleka Wakati wa Usiku

**- Mwanzo 31-33**

Yakobo hakujua kwamba Raheli alikuwa amevitwaa vinyago vya baba yake, na Labani alipoingia kwenye hema la Raheli, "Raheli alikuwa amevitwaa vile vinyago ameviweka katika matandiko ya ngamia, na kuvikalia". Labani hakuviona na Raheli akadanganya kwa kusema, "siwezi kuinuka mbele yako, maana nimeshikwa na mambo ya kike". Yakobo akamkasirikia Labani na kusema, "Nayo ni nini dhambi yangu hata ukanifuata namna hii… umepapasa vyombo vyangu vyote, ni kitu gani ulichokiona cha nyumbani mwako?" Yakobo akarudi kuelezea ulaghai wa Labani kwenye malipo na kwamba mchana na usiku, baridi na jua kwa miaka 20 amemtumikia kwa uaminifu. Akasisitiza kwamba kama isingekuwa Mungu wa Ibrahimu na Isaka kuwa pamoja naye, angelimfukuza mikono mitupu. Basi Labani akakiri kwamba wake zake ni binti zake, na wanyama wale ni wake, basi akafanya agano la mapatano naye, wakaita mahali pale Mispa maana yake "Mungu atuangalie kati ya mimi na wewe, wakati tusipoonana. Akamwonya asiwatese binti zake. Wakachinja sadaka mlimani, wakala chakula pamoja na kukaa mkesha, kisha Labani aliondoka asubuhi akawabusu binti zake na kuwabariki, kisha akarejea nyumbani kwake. Raheli alikuwa na mimba ya Benyamini, mwana wa 12 wa Yakobo na alipojifungua, alifariki.

Familia hii ilikuwa na mivunjiko mingi, madada, kaka, mama, baba mkwe nk. Mashindano kati ya ndugu, mitala, wivu, magomvi, kutawalana, hongo, hasira - yote hayo! Yakobo alikuwa amewalaghai wengine na sasa kibao kilikuwa kimegeuzwa kwake, Tunapomwamini Mungu kututimizia mahitaji yetu, tunapata usalama wa moyoni na furaha ambayo haiwezi kupatikana kwa kuwatumia au kuwadhibiti wengine. Utambulisho wetu wenye kutuletea furaha, msingi wake wapaswa utoke kwa Bwana na si kwa wanadamu.

Yakobo akashika njia yake na Malaika wa Mungu wakakutana naye, akasema, "Hili ni jeshi la Mungu". Akiwa na hofu juu ya ndugu yake Esau, Yakobo alituma ujumbe katika nchi ya Seiri au nyika ya Edomu na kusema, "mwambieni bwana wangu Esau, hivi ndivyo asemavyo mtumwa wako, Yakobo, nimekaa ugenini kwa Labani na kukawia huko hata sasa. Nami nina ng'ombe, punda, kondoo, watumwa na vijakazi, nami nimepeleka watu nimpashe bwana wangu habari nipate neema machoni pako". Basi, alipopata ujumbe akaja kumlaki na watu 400 pamoja naye. Yakobo akaogopa sana na kufadhaika, akagawanya watu waliopo naye akisema kwamba Esau akilipiga kundi moja, jingine litaokoka. Mke aliyempenda alimweka mwisho, na wengine aliwaweka mbele zaidi. Kweli mambo ya kuoa wake wengi yanaonesha chuki, au upendeleo wa wazi wazi. Basi Yakobo, akakaa mahali pa faragha ili aombe, na kumwambia Mungu, "Bwana uliyeniambia rudi uende mpaka nchi yako na kwa jamaa zako, Nami nitakutendea mema, mimi

sistahili hata kidogo hizo rehema zote, na kweli yote uliyomfanyia mtumwa wako". Akasema alivuka mto kwenda Harani bila kitu na sasa Mungu amembariki. Akamsihi Mungu amwokoe na mkono wa ndugu yake Esau, yeye na familia yake. Akawaambia makundi, na familia yake na vijakazi watangulie na yeye akabaki akiomba.

Yakobo aliandaa zawadi kwa Esau, mbuzi 220, kondoo 220, ngamia 30 na wana wao, ngombe 50 na punda 30. Akawaambia watumwa wake wampatie Esau zawadi hizo. Akavuka mto Yaboki pamoja na familia yake. Akakaa peke yake usiku na mtu mmoja akashindana Naye mieleka hata alfajiri. Mtu huyo alipoona kwamba hamshindi alimtegua paja lake. Yule mtu alimwambia Yakobo niache niende maana kunapambazuka. Yakobo akasema, "sikuachi usiponibariki". Yule mtu akamwambia,



"Jina lako hutaitwa tena Yakobo, bali Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu nawe umeshinda". Kushinda yaonekana ni kutokata tamaa, kamwe! Yakobo ndiye baba wa taifa la Israeli. Yakobo alitaka kujua jina la yule mtu, naye akasema, "kwa nini waniuliza jina langu?" Alipaita mahali pale Penueli, maana yake, "Nimeonana na Mungu uso kwa uso na nafsi yangu imeokoka".

Kulipokuwa kumepambazuka, Yakobo alitembea akichechemea kwa sababu ya kutenguliwa uvungu wa paja. Kutokana na tukio hili, wana wa Israeli hawali nyama ya paja. Hata wewe mwambie Mungu leo, 'sitakuacha mpaka unibariki'. Mambo ya kiroho yanaeleweka na kutambulikana kwa jinsi ya rohoni. Yakobo ambaye alitoka akiwa mzima kabisa, sasa alirudi kwenye kambi ya watumishi wake na familia yake akiwa anachechemea. Nao wakamwuliza mbona unachechemea? Bila shaka akawajibu "ni matokeo ya baraka kuu!" Nafikiri kilikuwa ni kitendawili kwao, mpaka alipoelezea mambo yaliyotokea.

Yakobo aliinua macho yake na kumwona Esau anakuja na jeshi lake. Yakobo akaenda kwa Esau akainama mara saba. Esau alimlaki na kumkumbatia, na kumwangukia shingoni akambusu na wote wawili wakalia. Wanandugu hawa wakapatana. Bwana anasema, "Njooni tusemezane, dhambi zenu zijapokuwa nyekundu zitakuwa kama theluji." Yakobo alikuwa amesamehewa na Mungu na kaka yake pia. Esau akauliza kuwa watoto na wale wake ni wa nani, Yakobo akajibu "ni watoto Mungu alionipa mtumwa wako kwa neema Yake". Basi wanawe, wajakazi na wake zake walikaribia na kuinama. Esau akauliza ile zawadi ya makundi ya mifugo, Yakobo akasema, "tafadhali upokee zawadi yangu mkononi mwangu". Basi mapacha hawa wakasameheana. Walikuwa wameachana miaka 20 iliyopita. Mama yao alikuwa

amekufa. Yakobo alijutia udhalimu aliofanya. Alitumika muda mrefu kwa Labani huku akiwa ameacha mali nyingi nyumbani kwao. Mungu ni mwenye rehema na anasemehe dhambi. Lakini inabidi tusikie sauti yake na kubadilisha mwenendo wetu wa dhambi kwa kuungama na kuwa na toba ya kweli kwake Yeye.

Esau alitaka wasafiri pamoja lakini Yakobo alitoa udhuru kwamba ana watoto wachanga na mifugo ambao kama "wakiharakishwa siku moja watakufa wote". Akamwomba Esau atangulie tu. Esau akarudi kwake Seiri na Yakobo akaendelea kwenda Sukothi, kisha akafika Shekemu. Hapo alichimba kisima kile ambacho mwanamke Msamaria wa Yohana sura ya nne aliteka maji. Yakobo na Esau walikutana tena kwenye mazishi ya baba yao Isaka. Esau aliendelea kuishi Edomu. Hata leo mkikosana na kaka au dada yako, muombane msamaha na msameheane kwa kuwa hakuna aliyekamilika, wote tuna madhaifu.

Sababu mbili zilizofanya sala ya Yakobo iwe na nguvu sana: ni kwamba alimwomba Mungu rehema. Yesu anasema wale wanaokuja kwa Mungu wakimsihi, "Nihurumie mimi mwenye dhambi!" ndio ambao wanahesabiwa haki badala ya wale wanaokuja kudai "haki" kwa sababu ya "wema" wao (Luka 18: 10-14). Jingine ni Yakobo alitegemeza ombi lake juu ya ahadi za Mungu (Mwanzo 32: 10-12). Maombi yetu yanategemezwa na ahadi za Mungu. Heshima ya kiti Chake Mungu cha enzi imewekwa kwa utimilifu wa Neno Lake. Hakika hatuna muda kuangalia makosa ya Yakobo au ya watu wengine, bali kuamka na kuangalia mioyo yetu wenyewe. Tuchukue Bibilia zetu, na kwenda kwa Mungu kwa sala ya dhati. Tumuulize atufundishe kujijua nafsi zetu wenyewe, kuelewa udhaifu wetu, dhambi zetu na ujinga wetu, tukizingatia umilele. tumuulize atuonyeshe tunaposimama mbele za mbingu. Hii ni kazi ya mtu binafsi. Tusipumzike mchana wala usiku hadi tuna ushuhuda wa kupata ushindi. Hakika Mungu anaweza kufanya hata maadui zetu wawe marafiki, tusikate tamaa tunaposali.

*Sala ya Yesu ni rahisi/sahili, wazi, ya kina kwa kujumuisha kila kitu, lakini sio ndefu kiasi cha kukosa joto la kiroho (spiritless) kama yalivyo maombi makavukavu ambayo mara nyingi hutolewa hadharani. Maombi haya yasiyo na roho ndani yake bora yasitamkwe; kwani yanashindwa kubariki au kujenga, na ni mfumo tu bila nguvu muhimu.

---

Yakobo alipigana mieleka na nani? Kwa nini Mungu alibadilisha jina la Yakobo? Elezea jinsi Mapacha walivyokutana. Esau aliishi wapi? Je, kwa nini kupatana baada ya ugomvi ni muhimu? Nimeona baadhi ya shida hizi kwenye ukoo n afamilia yangu, tufanyeje tuonapo shida kama hizi kwenye familia zetu? Je, unakabiliana na mieleka gani leo? Je, mapambano mtu aliyo nayo yanaweza kuleta baraka? Kama vitu vilivyoanikwa nje kwenye rafu za jumba la makumbusho, ndivyo neema ya Mungu inavyoanikwa wazi kwetu na katika maisha ya Yakobo, unaweza kuelezea hili?


**SIKU YA 21**
**(Januari 21)**

# Yusufu na Ndugu Zake

**- Mwanzo 35-39**


Yakobo alipofika Kanaani, kule Bethlehemu ndipo Benyamini alizaliwa na mamaye Raheli alikufa mara tu baada ya kumzaa. Yakobo sasa alikuwa na wana 12 na binti mmoja. Binti huyu Dina alitoka ili kuwaona binti za nchi hii ya Shekemu, na mwana wa mkuu wa nchi alimtwaa na kulala naye (hakuna maelezo zaidi, ila tunaweza kusema alibakwa). Alimpenda Dina na kuwa tayari kumwoa ila alianza kwa hatua isiyo njema. Kutaka kuoa haitoi udhuru ya kupita njia ambayo ni ya dhambi. Na dhambi moja inasababisha nyingine, kwani watu wengi wa mji ule waliuwawa.Tukumbuke kwamba wasichana na hata wavulana wanakuwa hatarini wakienda miji ya wale wasiomtii Mungu bila wazazi wao. Mwana huyu wa mfalme mwishowe akamwambia baba yake ampe msichana huyu awe mke wake. Yakobo alisikia na vijana wake walipokuja wakasikitika na kukasirika. Shekemu alisema kwamba kijana wake yu tayari kumwoa Dina na washirikiane nao katika biashara na kwa ujirani. Akawa tayari kutoa mahari. Kwa hila watoto wa Yakobo wakasema kwamba watamtoa dada yao ikiwa watu hawa watatahiriwa. Walikubali kutahiriwa wote, na wakiwa bado na maumivu ya tohara, ndipo Lawi na Simeoni wakawaendea na panga zao, na kuua wanaume wote, wakamtwaa dada yao Dina na kutoka, wakichukia kitendo alichotendewa dada yao. Yakobo aliogopa akawaambia Simeoni na Lawi “mmenitaabisha na kunifanya ninuke vibaya kati ya watu wa nchi hii”. Yakobo alijua maana ya kusamehewa alipotenda dhambi, ila vijana wake hawakuwa wamejifunza bado. Yakobo anarudia tukio hili katika kutoa baraka kwa watoto wake. Hakika hasira isiyozuiliwa ni mbaya!

Mungu akamwambia Yakobo ahamie Betheli na Yakobo akawaambia watu wa nyumbani mwake watoe miungu migeni iliyoko kwao ili waende Betheli na kumfanyia Mungu madhabahu huko. Wakampa mapambo yote ya pete, heleni na bangili. Mungu akamtokea tena Yakobo na kumwambia kwamba “uzidi kuongezeka, taifa na kundi la mataifa watatoka viunoni kwako”. Yakobo akatoa sadaka na kupaita mahali pale Betheli.



Yusufu alikuwa ni mmoja wa wana wa Yakobo na baba yake alimpenda sana. Kaka zake walikuwa sasa ni watu wazima, na pengine hata walikuwa wameoa. Yusufu alipendwa kwa kuwa alikuwa mtoto mtiifu na kwamba mama yake

Raheli ndiye aliyekuwa mke mpendwa wa baba yake. Yusufu alimletea baba yao, habari mbaya za ndugu zake, na hili liliwakasirisha. Yakobo (Israeli) akamfanyia mwana wake wa uzeeni Yusufu kanzu nzuri ndefu ya rangi na ndugu zake wakaona baba yao anampenda kuliko wao, wakamchukia na wala hawakuweza kusema naye kwa amani. Baba alikuwa anafanya kosa la upendeleo ambalo lilifanywa pia na wazazi wake. Yusufu akaota ndoto, na kuwaambia ndugu zake, kwamba walikuwa wakifunga miganda shambani, na mganda wake ukaondoka na kusimama, na miganda ya ndugu zake ikazunguka na kuinama mbele ya mganda wake. Ndugu zake wakamkejeli "Je kweli utatumiliki sisi? Nawe utatutawala sisi?" wakazidi kumchukia kwa ajili ya ndoto na maneno yake. Akaota ndoto nyingine ambayo aliona jua, na mwezi na nyota kumi na moja zikimwinamia. Alipowaambia baba yake na ndugu zake, baba yake alimkemea na kusema ni ndoto gani hiyo?, Je! Mimi na mama yako na ndugu zako tutakuja tukusujudie hata nchi?" Ndugu zake walimchukia, ila baba yake alihifadhi maneno hayo moyoni. Kile kilichoanza kama ushindani wa mapenzi kati ya Raheli na Lea kiligeuka kuwa chuki dhidi ya Yusufu.Ndugu zake walienda kuchunga Shekemu, mwendo wa Km 75 hivi. Israeli akamwambia Yusufu aende kuwajulia hali na kuwapelekea chakula. Alikwenda akizunguka na kuulizia, na mtu mmoja alimwambia kuwa ndugu zake wako Dothani, kama Km 22 hivi. Yusufu aliwafuata ndugu zake huko Dothani. Ndugu zake walipomwona angali mbali walisemezana kuwa wamwue na kumtupa shimoni kisha waseme kwamba mnyama mkali amemla. Reubeni mzaliwa wa kwanza aliposikia akatoa pendekezo



la kumwokoa. Hakumpenda Yusufu, lakini pia hakutaka afe, hivyo akawaambia, "msimwage damu, mtupeni katika birika hili lililopo nyikani, wala msimguse, ili apate kumwokoa katika mikono yao, amrudishe kwa baba yake". Walimvua Yusufu kanzu yake, na wakamtupa kwenye shimo kavu. Walikaa kula chakula alicholeta pale pale alipokuwa bila kumwonea huruma. Wakainua macho na kuona Msafara wa Waishmaeli wafanyabiashara. Ndipo Yuda akawaambia ndugu zake "kwafaa nini kumwua ndugu yetu… haya tumwuze kwa hawa Waishmaeli, wala mikono yetu isimdhuru". Aliwakumbusha kuwa yeye ni ndugu yao, na damu yao. Walikubali na wakamwuza kwa Waishmaeli kwa vipande ishirini vya fedha. Yusufu akachukuliwa kwenda Misri.

Reubeni aliporudi shimoni akamkosa. Basi akararua nguo zake, na alipouliza ndugu zake wakamwambia. Yeye kama kaka yao mkubwa aliogopa kuwa angemwambia nini baba yake; basi walitwaa kanzu ya Yusufu, wakachinja mwanambuzi na kupakaa damu kwenye ile kanzu. Walimpelekea baba yao wakisema itambue kanzu hii. Akaitambua kuwa ni ya Yusufu, akasema, "mnyama mkali amemla bila shaka". Yakobo akararua mavazi yake, na kujivika gunia, na kumlilia mwanawe

siku nyingi. Wanawe wakamtuliza lakini alitakaa kutulizwa, akilia “La! nitamshukia mwanangu, nikisikitika, hata kaburini”. Yusufu aliuzwa kama mtumwa huko Misri kwa mtu aliyeitwa Potifa aliyekuwa mkuu wa Askari wa serikali ya Farao. Huzuni kubwa kwa kijana wa miaka 17. Pengine alilia machozi ya upweke usiku akimkumbuka baba yake na mdogo wake Benyamini, au hata mama yake aliyefariki. Wivu ni kitu kibaya na hasa kwa wanandugu, wivu watoka kwa Shetani. Kumbuka hakuna kama wewe, kila mtu anapendwa na BWANA. BWANA alikuwa pamoja na Yusufu akamfanikisha mambo yote mkononi mwake ‘kila alichoshika kikawa dhahabu’. Potifa akamweka awe msimazi wa nyumba yake kwa vyote vilivyomo nyumbani na shambani wala hakujua habari ya kitu cho chote isipokuwa chakula alichokula tu.

Yusufu alikuwa mtu wa sura nzuri, na mke wa Potifa akamtamani na kumwambia “lala nami”. Mama huyu alifanya dhambi ya kuvunja amri ya saba. Isitoshe, ni jambo la aibu kwenye utamaduni wa kawaida kwa msichana ‘kumfukuzia mvulana,’ hata kama alikuwa hajaolewa, ingemfanya ‘ashuke bei’. Kisa hiki kinatoa msingi wa mahusiano ya ngono kwenye Agano la Kale na Jipya. Tendo la ndoa ni kati ya mke na mume tu. Basi Yusufu akakataa na kusema; Bwana wake Potifa amemwamini kwa kila kitu, na hakumzuilia kitu cho chote isipokuwa, “wewe kwa kuwa wewe u mkewe. Nitafanyeje ubaya huu mkubwa nimkose Mungu?” Mke wa Potifa akaendelea kusisitiza haya siku baada ya siku, naye hakumsikia alale naye au aongee naye. Siku moja mwanamke huyu alishika nguo ya Yusufu kwa nguvu, akisema “lala nami”. Kitendo hiki kinaweza kuitwa ubakaji kwa namna fulani au kumtweza mtu kwa nguvu ili ufanye naye dhambi. Yusufu alikimbia na kuaicha nguo yake.

Si waoga tu wakimbiao. Kukimbia dhambi ni ushujaa. Yule mwanamke akaita watu wa nyumbani mwake akidanganya kwa kusema, “angalieni ametuletea mtu Mwebrania atufanyie dhihaka, ameingia kwangu ili alale nami, nikalia kwa sauti kuu… aliiacha nguo yake kwangu, akakimbia, akatoka nje”. Akamwambia mume wake alipokuja akimwonyesha ile nguo. Hasira ya Potifa iliwaka, na akamtia Yusufu gerezani kwa wafungwa wa mfalme. Nafikiri, walijua kwamba haya yawezekana kuwa ya uongo, vinginevyo angeliuawa. Maskini Yusufu, alizidi kushangaa, mbona mambo yanazidi kuwa mabaya hivi? Bwana akawa pamoja na Yusufu akampa kibali machoni pa mkuu wa gereza, na akampa kuwa kiongozi, “wala mkuu wa gereza hakuangalia neno lililoko mkononi mwa Yusufu, kwa kuwa Bwana alikuwa pamoja naye. Bwana akayafanikisha yote aliyoyafanya”. Wapendwa hata nasi tukimpenda Mungu na kuyafanya Mapenzi Yake, atayafanikisha yote tunayofanya. Ni ahadi ambayo imehakikishwa hata kama mambo yanaonekana kuwa ni ya kukatisha tamaa. Kamwe usichoke kutenda mema kwa sababu ya ubaya wa watu. Linda njia zote za moyo, yale unayoona, unayosikia, unayonusa au kugusa ili usipotoke kutoka kwenye kuwa na moyo msafi na kujihusisha na urafiki wenye uovu kama mama Potifa alivyofanya. Uhusiano wa mapenzi au mahaba ya ndoa ni kati ya mtu na mkewe na siyo kila mtu. Na wakati ukifika wa kuchagua mwenzi wa maisha tunapaswa kufuata hatua za uchumba ambao unafuata maagizo ya Bwana. Kitendo kilichofanywa na mke wa Potifa ni ubakaji, jambo hili limetokea mahali pengine, na ni vyema likikutokea ukimbie, na kutaarifu wanaohusika ili upate msaada kutoka kwenye unyanyasaji wa jinsi hii. Mwombe Mungu akupe mpenyo wa

kutokea kutoka kwenye dhiki hii. Tuwakumbuke wale wanaoteseka gerezani isivyo haki au wanaoteseka kwa sababu ya uaminifu wao kwa Kristo.

Masihi hakutoka kwenye familia ya watakatifu na hilo limekuwa somo la kustaajabisha kwa wengi, na limempa nafasi watu makafiri kuidhihaki Biblia. Lakini hili ni mojawapo ya uthibitisho wenye nguvu zaidi wa Ukweli wa Maandiko, kwamba hakuna kinachofichwa humo, na wala dhambi za wahusika wake wakuu haziwekwi mvunguni. Akili za wanadamu zina ubaguzi kiasi kwamba haiwezekani kwa historia ya wanadamu kutokuwa na udanganyifu wa aina fulani. Ikiwa Biblia ingeandikwa na watu wasioongozwa na Roho wa Mungu, bila shaka ingeonyesha tabia za watu mashuhuri au wanaoheshimiwa kwa njia ya udanganyifu, kama vile tunavyoona kwenye usomaji wa baadhi ya wasifu kwenye mazishi. Lakini kama ilivyo, tuna rekodi sahihi ya maisha yao.

*Maombi yanayotolewa hadharani yanapaswa kuwa mafupi na kwenda kwenye pointi yaani yaguse vipengele vinavyohusika. MUNGU hatuhitaji tufanye msimu wa ibada kuwa wa kuchosha kwa maombi marefu. Dakika chache zinatosha kwa ombi lolote la kawaida la umma kumjulisha Mungu matamanio yetu.

---

Kwa nini ni hatari watoto kuingia majumbani mwa watu bila usimamizi? Kwa nini Yusufu alipendwa? Yusufu aliota ndoto gani? Kwa nini Yusufu alitumwa kwenda kwa kaka zake? Mke wa Potifa alikuwa na uovu gani? Kwa nini Yusufu hakufanya vile alivyotaka? Je, jambo gani lilitokea kwa Yusufu alipokuwa jela? Kwanini mahaba nje ya ndoa ni dhambi? Hasira kifuani mwa Lawi na Simeoni inatufundisha nini? “Kunyakuliwa kwa wasichana na wafalme au watoto wao, hakufanyi hili kuwa siyo dhambi mbele za Mungu, kama vile ambavyo ndoa ya jinsia ilivyo mbele za Mungu”, unaweza kuelezea hili?

**SIKU YA 22**
**(Januari 22)**

# Yusufu Atoka Jela

**- Mwanzo 40-41**

Mnyweshaji na mwokaji wa mfalme wa Misri walikuwa wamefungwa kwenye hii jela kwa sababu walimkosa bwana wao. Mkuu wa jela aliweka watu hawa chini ya usimamizi wa Yusufu. Usiku mmoja waliota ndoto. Asubuhi yake, Yusufu aliona wamefadhaika, na akawauliza sababu ya nyuso zao kukunjamana. Walimwambia kuwa waliota ndoto, na wakashindwa kujua tafsiri yake. Basi Yusufu akawaambia wamwambie ndoto zao. Akawaambia anayeweza kutoa tafsiri ya ndoto ni Mungu wa mbinguni. Alimpa Mungu utukufu, na wala hakujisifu kwamba ni yeye anayejua. Hii nadra ulimwenguni leo maana wengi wanadhani 'wanajua'. Ukijaribu kuwaeleza kitu, kabla hujamaliza wanasema "najua".

Mnyweshaji akasema kwenye ndoto, aliona mzabibu wenye matawi matatu uko mbele yake; mzabibu huu ulimea na kuchanua, na vishada vyake vilitoa zabibu zilizoiva. "Kikombe cha Farao kilikuwa mikononi mwangu, nikazitwaa zabibu, nikazikamua katika kikombe cha Farao nikampa Farao kikombe mkononi mwake". Yusufu akamwambia tafsiri ni kwamba katika siku tatu Farao atakurudishia kazi yako nawe utampa Farao kikombe mkononi mwake kama mwanzo. Alimsihi huyu mnyweshaji amkumbuke akiwa huko kwenye 'ikulu' ya mfalme, kwa kumtaja, na kumtoa jela, akamwambia, "kwa sababu niliibiwa toka nchi ya Waebrania, wala hapa sikutenda neno lolote hata wanitie gerezani". Naye wa pili, akasema kuwa kwenye ndoto aliona nyungo tatu za mikate myeupe kwenye kichwa chake. Nyungo hizo zilikuwa na kila chakula kwa Farao cha kuoka, na ndege wakavila katika ungo juu ya kichwa chake. Yusufu alitoa tafsiri kwa kusema kwamba katika siku tatu, Farao atamkata kichwa chake na kumtundika juu ya mti, na ndege watakula nyama yake. Baada ya siku tatu, Farao alifanya sikukuu ya kuzaliwa kwake, akafanya karamu na kualika watu na akafanya vilevile kama Yusufu alivyotafsiri zile ndoto. Hii ndiyo 'karamu ya kuzaliwa' ya kwanza kuandikwa kwenye Biblia! Mkuu wa wanyeshaji alipoenda ikulu hakumkumbuka Yusufu tena. Je, wewe hukumbuka waliokutendea wema? Wema hauozi tunaambiwa, hebu usioze mioyoni mwetu pia! Hakika Yusufu alijali wengine, japokuwa alikuwa na shida zake mwenyewe.

Basi baada ya miaka mitatu Farao aliota ndoto. Aliona amesimama kando ya mto na ng'ombe saba wazuri na wanono walipanda toka mtoni wakila nyasi. Kisha ng'ombe saba wengine wabaya na waliokonda walipanda na wakasimama karibu na wale ngombe ukingoni mwa mto. Wale ng'ombe wabaya wakawala wale wanono lakini hawakunenepa. Farao aliamka na kisha akalala tena na kuota ndoto ya pili. Aliona masuke saba makubwa na mema yaliyomea kwenye bua moja, na kisha akaona masuke saba membamba yamekaushwa na upepo wa mashariki

yalitokeza na kuyala yale masuke saba makubwa yaliyojaa. Farao aliamka na

kugundua kuwa ni ndoto tu, lakini roho yake ilifadhaika na asubuhi aliwaita waganga wote wa Misri na watu wenye hekima, ambao wengi wao walikuwa wachawi. Aliwahadithia ndoto na kuwaambia wamtafsirie. Ndipo mkuu wa wanyeshwaji akamkumbuka Mwebrania kiongozi aliyewatafsiria ndoto na kuwaambia kisa cha alivyotafsiriwa ndoto na mwenzake na tafsiri ikawa kweli. Farao alipeleka watu na kumwita Yusufu; nao wakamleta upesi kutoka gerezani, akanyoa na kubadili nguo zake na akasimama mbele ya mfalme. Farao alimwambia Yusufu ndoto yake na kwamba hakuna aliyeweza kutafsiri. Yusufu akajibu, "Si mimi, Mungu atampa Farao majibu ya amani". Yusufu akasema Mungu amemwonyesha Farao atavyofanya karibuni, wale ng'ombe saba ni miaka saba ya neema ya nchi na wale ng'ombe saba dhaifu ni miaka saba ya njaa. Akaeleza kwamba itakuja miaka saba ya shibe, na kisha miaka saba ya njaa, na ile shibe yote haitajulikana katika nchi kwa uzito wa njaa.



Akamwambia Farao ndoto hii imekuja mara mbili ikionesha kuwa Mungu amelithibisha Neno Lake na atalitimiza upesi. Akampa Farao maarifa ya kuweka akiba ya 1/5 ya mavuno yote kwa miaka saba ya shibe na kukilinda kuwa chakula katika miji, kwa ajili ya hiyo miaka saba ya njaa. Neno hili likawa jema machoni pa Farao, akawa mnyenyekevu na akawaambia watumwa wake, "Tupate wapi mtu kama huyu, mwenye Roho ya Mungu ndani yake?" Basi akampa Yusufu afanye kazi hiyo, akamwambia, "Nimekuweka juu ya nchi yote ya Misri". Akavua pete mkononi mwake akaitia mkononi mwa Yusufu, na kumvika mavazi ya kitani nzuri na mkufu wa dhahabu shingoni mwake. Akampandisha kwenye gari lake la pili alilokuwa nalo. Watu wakashangilia". Farao akampa mamlaka na kumwita Yusufu - Safenath-panea na kumwoza binti wa Kuhani wa Oni, aitwaye Asenathi. Kweli Mungu hana upendeleo, aweza kumpa ndoto hata mtu asiyemjua vyema kama Farao, hasa akifanyia watu wema na kusikia sauti ya Mungu, basi anabarikiwa kwa jinsi ya ajabu! Yusufu alikuwa na miaka 30 alipowekwa kuwa makamu wa Farao akienda huko na huko katika nchi ya Misri akikusanya akiba ya chakula kingi mno, kisicho na hesabu, ile miaka saba. Yusufu akapata wana wawili, akawaita Manase maana yake Mungu amenisahahulisha taabu zangu zote, na nyumba ya baba yangu, na wa pili akamwita Efraimu, maana yake Mungu amenipa uzazi katika nchi ya mateso yangu. Kweli, Mungu ni mwaminifu na wa upendo. Miaka saba ya shibe ikaisha na ikaja miaka ya njaa. Watu wakamlilia Farao ili awapatie chakula lakini aliwaambia waende kwa Yusufu na wafanye atakavyowaambia. Njaa hiyo nzito, ilikuwa ya dunia nzima iliyojulikana na watu. Watu wa nchi zingine walikuja

pia ili wanunue nafaka, kwa ajili ya chakula. Kweli hata leo inabidi tusome Neno la Mungu, ili kujiwekea akiba, kwani njaa inakuja, siku ambazo Neno la Mungu litakuwa halipatikani, bali tukiweka akiba litatusaidia. Tunaona uvumilivu wa Yusufu, hakusema "kwa nini mimi ndiyo napata shida zote hizi", bali aliendelea kumtegemea Mungu. Aliendelea kufanya kazi kwa uadilifu, japo alikuwa ameonewa. Mara nyingi tukionewa huwa tunakuwa wavivu kufanya kazi kwa yule bosi. Yusufu ambaye alikuwa mseja, aliendelea kuwa mwaminifu kwa Mungu, ni afadhali zaidi kuepuka dhambi kwanza kuliko kulazimika kutubu kwa huzuni baadaye. Wakati wowote tunapojaribiwa kutenda dhambi, malaika hutazama kuona tutafanya nini. Wanafurahi tunapokataa kuingia dhambini, lakini wanapata huzuni tunapoanguka katika jaribu. Majaribu mengi makubwa tunayokumbana nayo yameundwa na Shetani kuharibu mpango ambao Mungu anao kwa ajili yetu, kwani mpango Wake kwetu unaweza kutimizwa tu ikiwa tutabaki waaminifu Kwake Nasi tupatapo shida, tuzidi kumtegemea Mungu na kusali.

Ikiwa wewe ni mseja, endelea kuwa mwaminifu kwa Mungu. Ikiwa umeolewa, ongeza kwa hilo, endelea kuwa mwaminifu kwa mke wako. Wewe ni afadhali zaidi kuepuka dhambi kwanza kuliko kulazimika kutubu kwa huzuni baadaye. Kisa hiki kinafanana kidogo na kile cha Daniel na mfalme Nebukadneza kwani Mungu huwatunza watu Wake, na huwafunulia yahusuyo wakati ujao. Hata leo Mungu bado tuna kazi ya kufanya kabla ya kwenda nyumbani, na tunaweza kuwa na ushawishi mkubwa ikiwa tunamwakilisha Mungu kwa unyenyekevu.

*Maombi yetu na mikutano ya kijamii vinapaswa kuwa nyakati za msaada maalum na kutia moyo. Kila mmoja ana kazi ya kufanya ili mikusanyiko hii iwe ya kupendeza na yenye faida iwezekanavyo. Hii inaweza kufanywa vizuri kwa kuwa na uzoefu mpya kila siku katika mambo ya MUNGU, na kwa kutosita kusema juu ya upendo Wake katika makusanyiko ya watu Wake. Msiporuhusu giza au ukafiri kuingia mioyoni mwenu, havitadhihirika katika mikutano yenu.

---

Kwa nini Yusufu alikuwa bado na tumaini alipokuwa jela? Kwa nini Farao alitaka Yusufu aletwe? Yusufu alijuaje ndoto ya Farao? Farao alimfanyia nini Yusufu? Je, Yusufu alikuwa na furaha kutoka jela? Kwa nini Misri ilikuwa na chakula wakati nchi zingine zilikuwa hazina chakula? Ni nani alihakikisha chakula kinatunzwa Misri? Kwanini uchawi ni dhambi?

**SIKU YA 23**
**(Januari 23)**

# Wana wa Yakobo Waenda Kununua Nafaka

**- *Mwanzo 42 –43***



Yakobo alipoona njaa inazidi, alituma wanawe wakanunue chakula Misri ili wasife. Benyamini alibaki nyumbani, ili 'mabaya yasimpate'. Wana wa Israeli walipofika Misri, Yusufu akiwa ndiye aliyewauzia chakula, aliwatambua. Akasema nao kwa maneno makali kwa kuwatisha, "mmetoka wapi nyinyi?" Wakajibu kuwa wametoka Kanaani na wamekuja kununua chakula. Wao hawakumtambua, na akakumbuka zile ndoto alizoota, akawaambia "wapelelezi ... mmekuja kuuona utupu wa nchi". Wakajibu, la! tulikuja kununua chakula. Wakajieleza kwamba wao ni wana kumi na wawili wa mtu mmoja huko Kanaani, na ndugu yao mdogo yupo pamoja na baba yao, na mwingine (wakimaanisha Yusufu) hayupo. Basi aliwatishia kwa kusema watabainika kwa upelelezi wao, na hatawaruhusu watoke mpaka walete ndugu yao mdogo Benyamini. Akamtuma mmoja amlete Benyamini, na wengine wakae kifungoni ili ahakikishe 'maneno yao kama ni ya kweli, kama aishivyo Farao'. Siku ya tatu alisema wafanye hivi ili wakaishi, maana yeye anamcha Mungu. Walikubali ndugu yao mmoja afungwe gerezani, na wengine wamlete yule mdogo, na kuwapelekea ndugu zao chakula. Wale ndugu walisemezana huku dhamira zikiwashitaki, "kweli sisi tulimkosa ndugu yetu, kwa kuwa tuliona shida ya roho yake, alipotusihi, wala hatukusikia kwa hiyo shida hii imetupata". Reubeni

akawakumbusha, “sikuwaambia nikisema msimkose kijana? Wala hamkusikia, kwa hiyo damu yake inatakwa tena”. Tunapofanya uovu, unatusuta na kutushitaki mpaka pale tunapojutia makosa, tunapoungama, na kubadili njia zetu mbovu. Japo Walikuwa hawajamwambia baba yao kweli yote, mambo yalikuwa wazi.

Sasa walikuwa wanaanza kubadilika tabia zao za ukatili. Mungu alitumia njia hii ili kuwasaidia. Hawakujua kwamba Yusufu anaelewa kila wanachokisema. Yusufu, akajitenga nao akaenda akalia, kisha akawarudia na kumchukua Simeoni miongoni mwao na akamfunga mbele ya macho yao. Yusufu akawaambia watenda kazi wajaze vyombo vya ndugu zake na magunia yao na nafaka, na akawapa chakula cha njiani. Mizigo yao ilipojaa walipanda punda zao na kuanza safari kuelekea nyumbani, lakini walipofika njiani, mmoja wao alifungua gunia lake ili ampe punda chakula mara aliona fedha yake juu ya gunia. Alipowaambia nduguze, walitazamana na mioyo yao ilizimia, wakatetemeka wakisema, “Ni nini hii Mungu aliyotutendea”. Basi walipofika kwa baba yao walimweleza yaliyotokea Misri, na wakasema yule makamu wa Farao alisema nao kwa maneno makali, akisema wao ni wapelelezi. Wakamweleza kuwa walimwacha Simeoni huko. Walielezea pia walivyorudishiwa fedha kwenye magunia yao, nao wote na baba yao wakaingiwa na hofu. Yakobo akaona ni mengi yamempata na akawa anawaza, ‘sasa Yusufu ameenda, Simeoni pia na sasa mnataka kumchukua Benyamini’. Reubeni akamwambia baba yake awaruhusu waende tena maana njaa ilizidi na wangekufa. Akamwambia babaye, “uwaue wanangu wawili, nisipowarudisha kwako”. Hii haikuwa na maana, kwani wanawe wawili ni wajukuu wa Yakobo, wangemtia huzuni kama watoto wake tu! Yakobo akalalama kwamba “mabaya yakimpata katika njia aliyoiendea ndipo mtakaposhusha mvi zangu kwa sikitiko mpaka kaburini.” Hakika kila familia au wanandugu wanapatwa na shida na huzuni, jibu ni kumwona Mungu atusaidie migogoro yetu, na changamoto zote za dhambi, kwani hakuna aliyeachwa salama, hata nami sasa katika familia yangu ninapitia mgogoro mkubwa na ninamlilia machozi Mungu.

Kwa vile njaa ilikuwa nzito, wangekufa wote, na walikuwa familia ya watu 70; basi Yakobo akakubali warudi Misri kwenda kununua chakula kidogo. Yuda akasema Makamu wa Farao alisema hawataona uso wake mpaka Benyamini aende nao, hivyo ni lazima waende naye la sivyo wakae tu nyumbani. Yakobo akasikitika kwamba wamemwambia yule mtu kuhusu Benyamini, wakajibu kwamba aliwahoji sana, nao hawakutaka kusema uongo, maana hata hivyo hawakujua kwamba angesema waje naye. Yuda akachukua udhamini wa ndugu yake Benyamini na kuzungumza na baba yake kama kiongozi wao, baba yao akakubali na wakashuka huko na zawadi kwa Yusufu kama Zeri, ubani, asali, manemane na lozi. Wakachukua pesa maradufu, zile walizorudishiwa ili wazirudishe. Wakamchukua Benyamini pia, na Yakobo akasema, “Mungu Mwenyezi awape rehema usoni pa mtu yule ili awafungulie ndugu yenu huyo mwingine na Benyamini”. Walitwaa vitu vyao na wakashuka Misri na wakasimama tena mbele ya Yusufu. Yusufu akamwambia msimamizi wa nyumba awalete wale ndugu kwenye nyumba yake na akawachinjia na kuwaandalia rasmi, ili wale pamoja naye adhuhuri. Walipofika kwa Yusufu waliogopa wakifikiri wanakuja kwa mashtaka ya zile fedha walizorudishiwa kwenye magunia yao. Wakadhani kuwa wangelikuwa watumwa na punda zao. Wakaanza

kujitetea kwa yule msimamizi, na kusema wamezileta zile pesa walizozikuta kwenye chakula chao. Msimamizi aliwatia moyo "Amani iwe kwenu, msiogope, Mungu wenu, Naye ni Mungu wa Baba yenu, amewapa akiba katika magunia yenu, fedha zenu ziliniwasilia". Akawatolea Simeoni ambaye pengine kizimbani alipata muda wa kufikiri ukatili wake wa kuua kijiji kizima. Msimamizi aliwatawadha miguu na kuwapa punda zao chakula.

Yusufu alipokuja walimpa zawadi, na kumsujudia mpaka nchi. Kweli ndoto zake zilikuwa zimetimia bila wao kujua! Aliwauliza hali ya baba yao na wakasema hajambo na yuko hai. Wakainama tena wakasujudu. Akamwangalia Benyamini mdogo wake wa tumbo moja na kuwauliza kama huyu ndiye mdogo wao, na kumwambia Benyamini "Mungu akufadhili mwanangu". Kweli ndoa za wake wengi zinasababisha ndugu wa mama tofauti kuwa na mafarakano mengi. Yusufu akafanya hima akaingia chumbani alie humo, kisha alinawa uso na kutoka. Aliagiza chakula kiletwe, na alikuwa mwenyewe na nduguze, kwa kuwa Wamisiri wenyewe kama destruí yao ilivyokuwa hawakula na Waebrania. Aliwapanga ndugu zake kuanzia mzaliwa wa kwanza mpaka wa mwisho nao wakastaajabu kwamba alijuaje? Benyamini akapata chakula mara tano zaidi ya ndugu zake.

**MAONI**

Ezra 5 ilituonyesha jinsi watu wa Israeli walivyohatarisha sifa zao na mamlaka ya kutawala ya siku zao ili kumtii Mungu. Ezra 6 inafunua matokeo. Badala ya kusimamisha kazi, kama Tatnai na marafiki zake walivyotarajia, uchunguzi wao ulimchochea mfalme kuwasaidia Waisraeli kufuata amri ya Mungu ya kujenga hekalu.

Kwa kutiwa moyo na Hagai na Zekaria, manabii wa siku hizo, watu walimaliza kazi hiyo kwa mafanikio. Lakini sio tu kazi yao ilikamilishwa - mioyo yao ilikuwa sawa na Mungu, pia. Mstari wa 16 unatuambia kwamba 'waliiweka wakfu nyumba hii ya Mungu kwa furaha. Mistari ya 20-22 inaripoti kwamba makuhani na Walawi wote walikuwa safi na kwamba Waisraeli ambao "walikuwa wamejitenga… kwa kuwa Bwana alikuwa amewafurahisha."

Mungu Yule Yule tunayemtumikia leo. Tunapojitolea kwa kutii maagizo ambayo tumepokea kutoka Kwake, atatutumia kumaliza kazi Yake, hata kama hali za mateso au kupigwa marufuku zitainua pembe zake. Hakuna mtu anayeweza kuharibu mpango wa Mungu kwa mtu mwingine. Hata Shetani hawezi. Mtu pekee ndiye anayeweza kuharibu mpango wa Mungu kwa mtoto wa Mungu, yaani mtu mwenyewe-kwa maisha ya kutomtii Mungu au kutojenga hekalu la mwili wake. Ikiwa Mungu anapendezwa nasi haijalishi mtu yeyote anasema nini au anafikiria nini juu yetu. Kisa cha Yusufu kinatufunulia kwamba Tabia ina thamani zaidi. Kwa nini Mungu hakumpa Farao ndoto hiyo mwaka mmoja mapema au baadaye? Mungu ana ratiba Yake kuhusu mitihani yetu. Wanadamu wanaweza kutusahau lakini Yeye kamwe hatatusahau. Katika ujuzi Wake - yote ya mbele na nyuma, anazingatia kusahau na kutotenda kwa mwanadamu katika kupanga wakati Yeye atatukomboa kutoka kwenye mtanziko wetu. Hata tunapofikiri amechelewa kwa siku nne, bado ametunza wakati (Yohana 11). Kwa habari ya Yusufu, Mungu

alikuwa mekusudia kwamba angeanza kazi yake katika serikali ya Farao akiwa na umri wa miaka thelathini, kama Yesu ambaye alianza huduma Yake akiwa na umri wa miaka thelathini, kwa kuwa alifananishwa na Yesu katika mambo mengi. "Kuchelewa" kwa miaka miwili kulimleta kwenye umri huo. Mwisho wa siku, mambo yote yalifanya kazi pamoja kwa manufaa yake. Ndivyo ilivyo kwa kila mtoto wa Mungu! "Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi Lake. Bwana anaposonga mbele, hakuna anayeweza kumzuia, Hivi karibuni Atasonga mbele kumalizia kutangaza injili na hakuna nguvu au kizuizi kinachoweza kumkwamisha. "Kwa maana Bwana atalitekeleza Neno Lake juu ya nchi, akilimaliza na kulikata." (Rum. 9:28). Amina! Songa mbele Bwana! Na tusaidie tuwemo ndani ya treni Yako. Basi, tuseme nini juu ya mambo haya? Mungu akiwa upande wetu, ni nani aliye juu yetu?

*Mikutano yetu inapaswa ifanywe kuwa ya kuvutia sana. Inapaswa kuwa na angahewa la manukato ya mbinguni. Wala kusiwe na hotuba ndefu, kavukavu na maombi ya mazoea, kwa sababu tu ya kutimiza muda .

---


Kwa nini Yusufu alitia hofu ndugu zake? (kashikashi au chokochoko) Je, ndugu zake walisikiaje? Je, walimwacha nani Misri? Kwa nini Yakobo hakutaka Benyamini aende na ndugu zake? Kwa nini Yusufu alitaka Benyamini aletwe? Kwa nini Yusufu alimpa vitu Benyamini zaidi ya wengine? Kwa nini Yakobo alitoa zawadi kwa mtawala wa Misri? Je! Familia ikipatwa na mgogoro au shida, zipi ni hatua kufuata?

**SIKU YA 24**
**(Januari 24)**

# Yakobo Akutana na Yusufu, Na Yusufu alipa mema kwa mabaya

**- *Mwanzo 44 na 45***

Yusufu alimwamuru msimamizi ajaze magunia yao chakula na atie fedha kinywani mwa magunia yao tena, na kikombe chake cha fedha akitie katika guniani la Benyamini. Kulipopambazuka, walipewa ruhusa kurudi kwao na punda zao. Wakitoka tu nje ya mji, Yusufu alimwambia msimamizi awafuate na kuwaambia "Kwa nini mmelipa mabaya kwa mema? Je, kikombe hiki, sicho anyweacho bwana wangu?" Alipowafikia na kuwaambia haya, walisema hawakuchukua fedha kinywani mwa gunia isipokuwa zile wamezirudisha, na atakayeonekana na kikombe cha dhahabu basi na afe na wao wako radhi kuwa watumwa wa Yusufu. Walishuka kwenye punda haraka na kufungua, ndipo wakaona kikombe kwenye gunia na Benyamini, na wakararua nguo zao kwa huzuni na wakarudi mjini. Yuda na ndugu zake wakamwangukia Yusufu kifudifudi huku wakisema, "tusemeje! Tujivutieje haki? Mungu ameona uovu wa watumwa wako. Tazama sisi tu watumwa wa bwana wangu". Yusufu akasisitiza si wote bali Benyamini tu ambaye kikombe kilionekana kwake, ndiye atakuwa mtumwa, bali wengine enendeni kwa amani



kwa baba yenu. Yusufu alitaka awajaribu kama bado wana ubaguzi kwa watoto wa mama yake. Yuda akasimama ili amkomboe Benyamini, akamweleza hali ya baba yao mzee na kwamba Benyamini ndiye mdogo mpendwa, na kaka yake alifariki, na sasa wasiposhuka na ndugu yao huyu, watashusha mvi zake na msiba kaburini. Wakamsihi amwachie Benyamini maana roho ya kijana imeshikamana na baba yao. Yuda akasema yeye ndiye mdhamini, na ndiye atakayechukua hatia asipomrudisha. Akamsihi Yusufu awe badala ya Benyamini akae ila kijana aende pamoja na nduguze, maana hakuna jinsi wanavyoweza kumwendea baba yao.

Yusufu akajua kweli ndugu zake wamebadilika, na kwamba wanampenda Benyamini na baba yao kwa dhati! Hakujizuia tena bali alipiga kelele na kusema, Wamisri wote watoke, ndipo alipojitambulisha kwa nduguze. Alipaza sauti, hata Wamisri wa nyumba ya Farao waliisikia. Alisema, "mimi ndimi Yusufu; baba yangu angali hai bado?" Ndugu hawa walikuwa wameshikwa na hofu na bumbuwazi. Yusufu akawaambia wamkaribie naye akasema, "mimi ni Yusufu ndugu yenu, ambaye mliniuza Misri. Basi msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu…maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu". Aliwabusu ndugu zake kwa upendo, Akawaeleza kwamba kuna miaka mitano zaidi ya njaa, kutokana na ndoto Farao aliyopewa na Mungu. Aliwaeleza jinsi alivyopata upendeleo wa Farao na kuwaambia yeye hana kisasi moyoni, "si ninyi mlionipeleka huku, ila Mungu, naye ameniweka kama baba kwa Farao na bwana katika nyumba yake yote, na mtawala katika nchi yote ya Misri". Aliwaambia wafanye hima wamlete baba yao Misri. Akawaambia wamweleze jinsi Mungu alivyombariki huko Misri, nao watakaa Gosheni pale mwisho wa mto Naili penye rutuba wakichunga mifugo yao na kulima. Akawaambia kwamba wamwambie baba yao 'wamemwona kweli'. Akahimiza waende na kumleta baba yao, kisha wamwambie kuwa Mungu amemweka kuwa mkuu katika nchi ya Misri, "hebu na ashuke asikawie". Kweli ni vigumu kwangu kusoma kisa hiki cha Yusufu bila kutoa machozi; upendo wa kweli husamehe.Hata huzuni iwe kiasi gani, na Mungu anakupa hekima ya kuwa na mahusiano mapya, yanawezekana siyo yale ya awali ila Mungu atakuonyesha, ila kusamehe ni muhimu, kwani asiyesamehe ni kama alinayekunywa sumu akitegemea yule mbaya wake ndiye atadhuriwa! Waliokufanyia ubaya katika hali zingine si lazima awe rafiki yako wa karibu (BF-Best friend) au umchukue kukaa naye nyumbani mwako, ila Mungu atakupa kusamehe na kutenda kadri ya mapenzi Yake.

Visa vya ajabu namna hii vya utendaji na wema wa Mungu viko vingi kwenye Maandiko. Mfano upekuzi uliotolewa na gavana Tatenai kwa hati ambayo ilifichwa, nayo ilipatikana na Mungu akamfanya Dario atoe amri ya kuidhinisha ujenzi uliositishwa miaka 13, Zaidi ya hayo, Dario alitoa wanyama wa kutolewa dhabihu kwenye huduma za hekalu. Kisha akaongeza: "Pia natoa amri kwamba yeyote atakayebadili amri hii, mti na ung'olewe kutoka katika nyumba yake naye atundikwe juu yake; na nyumba yake na iwe lundo la takataka kwa sababu hiyo. Hii ilipelekea kukamilishwa kwa hekalu kwa muda mfupi na rasilimali tele. Kwa mpango wa Mungu, wazee wa Kiyahudi, manabii wa Kiebrania, na wafalme wapagani wote walichangia kukamilisha kazi hiyo. Ndugu na dada zangu, ikiwa Mungu amepanda kitu moyoni mwenu endeleeni kukifanya. Mungu akiwa pamoja nasi ni nani awezaye kuwa juu yetu? Na kwa hivyo hekalu lilijengwa, kuwekwa wakfu na huduma za kila

siku na za kila mwaka zilianza tena ndani yake baada ya miaka sabini. Je, unaweza kuhisi hisia kali za wakati huo? Miaka ya uchungu, huzuni, na upweke inaachiliwa katika kwa kilio kilichosikika mbali. Je, Umewahi kupata hisia kali kama hii katika maisha yako na kuangua kilio? Ikiwa ndivyo, kulia kunasaidia afya, toa hisia hizo zote kali badala ya kujaribu kuziweka ndani ya chupa ya moyo. Yesu alilia alipokuwa njiani kuelekea kaburi la Lazaro. Yesu tayari alijua kile ambacho angefanya, lakini alihisi uchungu na huzuni ya Martha na Mariamu. Yesu, Mwokozi wetu mwenye upendo, anafahamu huzuni na machungu yetu. Nduguze Yusufu walikuwa wenye kujali na wenye huruma, hali ambayo ilikuwa tofauti kabisa na mtazamo wao walipomuuza utumwani. Na wakati Yuda alipojitolea kuchukuliwa kama mtumwa badala ya Benyamini ilikuwa ni uthibitisho zaidi kwamba walikuwa wamefanywa marekebisho. Nguvu ya Mungu iliyowarekebisha wanandugu hao, inapatikana kwa ajili yetu pia tunapotafuta uamsho na matengenezo. Hebu na tuendelee kusoma Biblia zetu na kuomba basi, kwa maana Biblia inasema, "Uwatakase kwa ile Kweli yako. Neno lako ni kweli."

*Omba, kisha; omba, nawe utapokea. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, ongezeko la imani. Kwa kila ombi la dhati jibu litakuja. Linaweza lisije vile vile unavyotamani, au kwa wakati unaolitafuta; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao utakidhi mahitaji yako kwa ubora zaidi. Maombi unayotoa katika upweke, katika uchovu, katika majaribio, MUNGU hujibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini daima kwa faida yako.

---

Je, wale wana wa Yakobo walifurahi kurudi tena Misri na kikombe? Kwa nini ilibidi warudi? Kwa nini Yusufu aliwaambia yeye ni nani? Walijisikiaje? Je, unajifunza kitu gani katika maisha ya wale ndugu 11?

**SIKU YA 25**
**(Januari 25)**

# Familia ya Yakobo Yaenda Misri

***- Mwanzo 45 na 46***



Yusufu alianza na ndoto kubwa, ila akatupwa gerezani, na kisha akasingiziwa kumbaka mke wa bosi wake, sasa alikaa kwenye kiti cha makamu wa mfalme au raisi wa nchi. Hakika Mungu ndiye tumwachie kulipiza kisasi. Labda umekuwa na ndoto maisha yako yote ya kufanya jambo kubwa kwa ajili ya Mungu, lakini mipango yako imeharibika na umefikia mwisho wa tumaini lako. Labda inaonekana kama Mungu amekuacha. Lakini Mungu hajasahau ndoto aliyoweka moyoni mwako, kwani ni ndoto yake pia. Kama vile alivyofanya kwa Yusufu, Mungu anapigana vita vyako, akifanya kusudi Lake liwe kweli maishani mwako. Basi Farao alipojua kuwa ndugu za Yusufu wamekuja akamwambia Yusufu awachukue ndugu zake na baba yake naye atawapa mema ya Misri na kula unono wa nchi. Akawapa magari ili wakamchukue baba yao, akawaambia mema ya nchi ya Misri ni yao. Wakapewa chakula cha njiani, na fedha na punda kumi waliochukua nafaka, mikate na chakula. Yusufu akawakumbusha tena "msigombane njiani", akifikiri pengine wataona wivu kwa vile Benjamini alipewa mavazi matano na fedha mia tatu. Ilichukua wiki mbili kwa mwendo wa mguu kutoka Misri mpaka Kanaani, umbali wa km 450 hivi. Walipofika kwa baba yao, walimshangaza na kisa cha 'Yusufu aliye hai', na kuwa ni mtu mkuu katika nchi yote ya Misri. Moyo wake ukazimia, kwani hakuwaamini. Ukawa muda wa kukiri uovu wao, nao wakapata kuwa huru moyoni! Wakamwambia yote Yusufu aliyowaambia, na alipoona magari ya Farao waliyopewa ili kumchukua, roho yake ikafufuka naye akasema, "yatosha!

Yusufu mwanangu angali hai; nitakwenda nionane naye kabla sijafa. Basi Yakobo akasafiri, na njiani akatoa sadaka kwa Mungu.

Mungu akanena na Israeli kwa ndoto usiku, “Mimi ni Mungu, Mungu wa baba yako, usiogope kushuka mpaka Misri, maana nitakufanya uwe taifa kubwa huko, Mimi nitashuka pamoja nawe mpaka Misri.” Wakaenda familia yote na mifugo yao. Jumla familia ya Yakobo, wajukuu, wake na watoto walikuwa watu 70. Yuda akaongoza msafara kwenda Misri, wakaenda mpaka Gosheni na Yusufu akaleta gari lake kumlaki Israeli baba yake na alipomwona alimwangukia shingoni na kulia kwa kitambo. Yakobo akaona kwamba sasa anaweza kufa, kwani macho yake yamemwona mwana wake mpendwa Yusufu, baada ya kutengana naye kwa miaka 13 hivi. Yusufu akampasha Farao habari, kwamba watu wake wamekuja na akasema ni wachungaji wa mifugo. Naye Farao alipowauliza walimwambia kwamba wao ni wafugaji na wakaomba awaruhusu wakae Gosheni kwani wamehamia kwake kwa ajili ya njaa. Basi Farao akasema, “Misri iko mbele yako, palipo pema pa nchi ukawalishe baba yako na ndugu zako”. Akaomba wale watu hodari wa kufuga, wana wa Israeli wamsaidie kuchunga wanyama wake. Yusufu akamleta baba yake mbele ya Farao akiwa na miaka 130. Yakobo akambariki Farao. Naamini Farao alimjua Mungu wa mbinguni kupitia kwa Makamu wake Yusufu. Huyu alikuwa ameishi maisha ya taabu toka ujanani na Mungu akamweka kivulini. Yusufu aliendelea kuwapatia chakula ndugu zake na Wamisri wakati wa njaa, akikusanya pesa na kuweka katika hazina ya Farao. Njaa ilipokuwa kubwa, Wamisiri walitoa farasi na wanyama wao ili wapate chakula na mwishowe walitoa hata ardhi yao.

Basi nchi yote ya Misri isipokuwa ile ya makuhani, ikawa mali ya Farao. Yusufu akawapa watu mbegu za kupanda, na walipovuna walimpa Farao 1/5, na iliyobaki 4/5 ikawa yao na watoto wao. Yakobo akaishi miaka 17 Misri, akamwita Yusufu na kumwambia ampe ahadi kwamba akifa atamzika kwenye kaburi la baba zake huko Makpela, naye Yusufu akamwapia. Basi Yakobo akawaita Manase na Efraimu watoto wa Yusufu ili awabariki. Yakobo akawachukua kama watoto wake na kutimiza kabila kumi na mbili za Israeli. Mara nyingi Yusufu na Dani walikuwa hawatajwi bali Efraimu na Manase. Macho ya Yakobo yalikuwa hayaoni kwa uzee. Aliwakumbatia wajukuu na kuwabusu. Akambariki Mdogo kama mzaliwa wa kwanza, na Yusufu alipojaribu kumzuia, baba yake alisema “atakuwa mkuu, lakini ndugu yake mdogo atakuwa mkuu kuliko yeye, na uzao wake utakuwa mwingi katika mataifa”. Aliendelea kusema “katika ninyi Waisraeli watabarikiwa, wakisema Mungu akufanye kama Efraimu na Manase”. Akamwambia Yusufu kuwa maisha yake yako ukingoni lakini Mungu atakuwa pamoja nao na siku moja atawarudisha nchi katika nchi ya baba zao, ile ya Kanaani. Yusufu alionekana kama ana uzaliwa fulani wa kwanza, kwa maana alikuwa kama kiongozi wa ndugu zake sasa, ila Yuda ndiyo ilikuwa sehemu yake aliyopewa kihalali, na japo alionekana kufanya makosa na hata dhambi nyuma, alikuwa ameungama.

Kisa cha Yusufu kinamwakilisha Masihi pia kwa namna fulani. Yesu Kristo alitendewa kama tunavyostahili, ili kwamba tuweze kutendewa kama alivyostahili kutendewa. Alihukumiwa kwa ajili ya dhambi zetu, ambazo Yeye hakuzishiriki, ili kwamba tuweze kuhesabiwa haki kwa haki Yake, ambayo sisi hatukuwa na sehemu nayo. Aliteseka

kwa kifo ambacho kilikuwa chetu, ili sisi tupate uzima ambao ulikuwa Wake. "Kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Kwa maisha Yake na kifo Chake, Kristo alipata zaidi ya urejeshaji kutoka kwenye uharibifu unaoletwa na dhambi. Lilikuwa ni kusudi la Shetani kuleta utengano wa milele kati ya Mungu na wanadamu; lakini katika Kristo tunakuwa tumeunganishwa karibu zaidi na Mungu kuliko kama tungekuwa kabla ya hatujaanguka. Katika kuchukua asili yetu, Mwokozi amejifungamanisha Mwenyewe na wanadamu kwa kifungo ambacho katu hakiwezi kuvunjwa. Tangu milele zote Ameunganishwa na sisi. Mungu aliupenda ulimwengu, hata Akamtoa Mwanawe pekee. Alimtoa sio tu ili kubeba dhambi zetu, na kufa kama kafara yetu; Alimtoa kwa ajili ya jamii iliyoanguka. Ili kutuhakikishia shauri Lake la amani lisilobadilika, Mungu alimtoa Mwanawe wa Pekee awe mmoja wa familia ya kibinadamu, ili kudumisha asili Yake ya kibinadamu milele.

*Mazungumzo ya muda mrefu na maombi marefu hayafai mahali popote, na haswa katika mkutano wa kijamii. Yanawachosha malaika, na vile vile watu wanaoyasikiliza. Maombi yetu yanapaswa kuwa mafupi, na ya moja kwa moja kwenye mada/pointi. Hebu Roho wa MUNGU ikae mioyoni mwa waabudio, Naye atafutilia mbali desturi zote na mambo duni (yanayoboesha).

---

Yakobo alionaje kwenda Misri? Alijuaje kwamba aende Misri? Alifika huko akiwa na miaka mingapi? Kwa nini Waisraeli walikaa Gosheni? Watoto wa Yusufu ni akina nani? Yakobo aliishi Misri miaka mingapi? Kanaani mpaka Misri ilikuwa umbali gani? Linganisha Kisa cha Yusufu na Masihi.

**SIKU YA 26**
**(Januari 26)**

# Yakobo Amaliza vyema kwa Kutoa Mibaraka kwa Wanawe

**- *Mwanzo 49 na 50***

Yakobo akawaita wanawe wakusanyike na akaanza kuwabariki. Jambo ambalo ni jema kwa kila mzazi kulifanya kila siku, yaani awabariki wanawe! Majina ya Biblia Hufichua Tabia wakati mwingine. Na wakati mwingine Majina mapya yaliyotewa/kubadilishwa kuendana na mhusika. Inafunua kuelewa maana halisi ya jina la kila kabila. Roho wa Mungu alimfunulia mzee huyu wa imani historia ya baadaye ya uzao wake. Akasema Rubeni kama mzaliwa wa kwanza, mwana wa ujanani wake mwenye nguvu amefanya vibaya kwa kulala na mama yake wa kambo Bilha na hivyo uzaliwa wa kwanza hautaenda kwake. Simeoni na Lawi kwa kuwa watu wa jeuri, na ukatilii kwa watu "nafsi yangu usiingie katika siri yao … ghadhabu yao na ilaaniwe, maana ilikuwa kali" na wote wakakosa uzaliwa wa kwanza. "Yuda ndugu zako watakusifu. Wana wa baba yako watakuinamia…Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, wala mfanya sheria katika miguu yake, hata atakapokuja Yeye mwenye milki". Yuda akapewa baraka kubwa ya kuwa Baba wa uzao wa Kristo. Zabuloni akaambiwa atakaa pwani ya bahari na kuegesha merikebu. "Isakari ni punda hodari" atakuwa mtumishi wa kazi ngumu. Dani atahukumu watu wake, ila atakuwa nyoka barabarani. Gadi jeshi litamsonga ila atawasonga mpaka visiginoni. Asheri chakula chake kitakuwa kinono na atatoa tunu za kifalme. Naftali atakuwa kama ayala aliyefunguliwa, atatoa maneno mazuri. Yusufu akapewa mibaraka ya vilindi vya bahari na ya maziwa na mibaraka mikuu ya kupita milima ya kale, "vitu vinavyotamanika vya vilima vya milele, na vikae juu ya kichwa cha Yusufu. Juu ya utosi wa kichwa chake aliye mkuu kati ya ndugu zake". Benyamini, atakuwa kama mbwa mwitu akila mawindo asubuhi na kugawanya mateka jioni. Akawaambia anaiendea nchi ya watu wote, yaani, kifo. Alipomaliza "akakunja miguu yake kitandani, akafa". Yusufu akamwangukia baba yake shingoni na kumlilia. Akaamuru wauweke mwili wake dawa ili usioze, Wamisri wakamlilia siku 70. Makabila ya Dan na Efraimu hayaonekani katika kitabu cha Ufunuo, yawezekana ni katika kutenda kwao makosa, yaliondolewa. Angalia Ufunuo 7.

Basi Yusufu akasema na Farao na kumwambia, "baba yangu aliniapisha…unizike katika kaburi langu nililojichimbia katika nchi ya Kanaani". Akamsihi amruhusu aende akamzike baba yake na kurudi. Farao akamruhusu naye akaenda na nduguze, watumwa na wazee wa Misri wakiacha watoto tu. Wakaomboleza maombolezo mazito na matanga ya siku saba, kisha wakamzika katika pango la Makpela. Kisha Yusufu akarudi Misri pamoja na ndugu zake. Ndugu zake bado walikuwa wanajisikia hatia na wakamtuma mmoja wao amwambie kwamba baba yao aliagiza akisema, "Yusufu… Naomba uwaachilie ndugu zako kosa lao na dhambi yao, maana walikutenda mabaya," sasa tunakuomba utuachilie kosa la watumwa wa Mungu

wa baba yako”. Yusufu akalia waliposemezana naye, nduguze wakamwangukia miguuni wakisema wao ni watumwa wake, wakiogopa kwamba baba yao amekufa na hivyo atawalipiza uovu waliomfanyia. Yusufu akawaambia kuwa yeye si Mungu, wasiogope, kwani wao walikusudia mabaya bali Mungu alikusudia mema, ili itokee kuokoa taifa kubwa. Akawaahidi kuwa atawalisha watoto wao na akawafariji na kusema nao vyema. Yusufu aliishi miaka 110, akaona vizazi vitatu vya watoto wake. Alipokaribia mwisho wa uhai wake, aliwaambia ndugu zake kuwa, “Mungu atawapandisha kutoka katika nchi hii mpaka nchi aliyowaapia Ibrahimu, na Isaka na Yakobo”. Basi akawasihi kuwa watakapokuwa wanaondoka, waipandishe mifupa yake huko pia. Hata nasi tumeahidiwa Kaanani ya mbinguni. Hebu tuangalie Mahesabu machache- idadi ya miaka Israeli ilikaa Misri. Yusufu aliuzwa Utumwani akiwa na umri wa miaka 17 hivi. Alipokuwa na umri wa miaka 30, akawa mkuu wa pili wa Misri. Akakaa miaka 93 huko Misri. Yakobo alikuja Misri alipokuwa na umri wa miaka 130 hivyo akaishi miaka 17 huko Misri. Lawi alitumia takribani miaka 42 huko Misri - aliishi miaka 137, miaka 9 baada ya kifo cha Yusufu. Kohathi aliishi miaka 133. Amramu aliishi miaka 137. Amramu alikuwa baba yake Musa. Musa mzaliwa wa Misri, aliyelelewa katika jumba la kifalme aliua akiwa na miaka 40 na akaishi jangwani miaka 40 zaidi. 93+9+133+137 = miaka 372. (Tukichukulia kwamba Kohathi na Amramu walikuwa watumwa maisha yao yote wakati wa utumwa ungekuwa miaka 270. Yusufu na Lawi hawakuwa utumwani.) Mambo zaidi yanahitajiwa kuzingatiwa, Endelea kufanya haya mahesabu…..! Kitabu cha Mwanzo ni matukio ya miaka takribani 2600! Toka kuumbwa kwa Adamu na Hawa, Mpaka kifo cha Yusufu. Hakuna kitabu cha Biblia kinachokua matukio ya miaka mingi kama hiki. Musa alikiandika akiwa anachunga Kondoo Midiani miaka ya Takribani 1400KK.

Jambo zuri ni kuwa familia hii ilipata fursa ya kuombana misamaha. Ni wangapi wameishi miaka mingi kwa majuto kwa kutotafuta msamaha. Familia nyingi zimetengana leo na zikakosa furaha kwa machozi, kutoelewana, chuki na uovu. Hata mtu anapotukosea tukiendelea kumchukia tutakuwa tumetenda uovu nasi tusifike Nchi ya Ahadi. Tumewambiwa “Iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, wenye kusameheana kama na Mungu anavyotusamehe kwaajili ya Kristo. Waefeso 4:32. Kitabu cha mwongozo wa Mungu kwetu kwa maisha ya kila siku (Biblia) ndiyo taa ya miguu yetu na mwanga wa njia yetu. Kamwe usipite siku bila hiyo taa! Je, unaweza kuhisi shangwe wakati wana wa Yakobo walipounganishwa tena? Ni kana kwamba Yosefu alikuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu!

Hebu wazia furaha isiyo na kifani katika asubuhi ya ufufuo wakati Yesu atakaporudi katika utukufu. Siku hiyo itakuwaje? Tutalia, lakini sio machozi ya huzuni, bali machozi ya furaha! Je, utamtafuta nani katika siku hiyo tukufu? Mapenzi ya Mungu yatatimia sikuzote kwMkutano unapaswa kufunguliwa kwenye saa iliyopangwa kadri inavyowezekana, iwe wamehudhuria wengi au wachache. Desturi au mapokeo na ubaridi uliokakamaa au uhafidhina unapaswa kuwekwa kando, na wote wanapaswa kuwajibika katika jukumu. Katika matukio ya kawaida kusiwe na maombi ya zaidi ya dakika kumi. Baada ya kuwepo mabadiliko la nafasi, na zoezi la uimbaji au mashauri limefurahiwa sawa, basi, ikiwa yeyote anahisi mzigo wa ombi, basi na aombe.

*Mkutano wa maombi unapaswa kufunguliwa kwenye saa iliyopangwa kadri inavyowezekana, iwe wamehudhuria wengi au wachache. Desturi au mapokeo na ubaridi uliokakamaa au uhafidhina unapaswa kuwekwa kando, na wote wanapaswa kuwajibika katika jukumu. Katika matukio ya kawaida kusiwe na maombi ya zaidi ya dakika kumi. Baada ya kuwepo mabadiliko la nafasi, na zoezi la uimbaji au mashauri limefurahiwa sawa, basi, ikiwa yeyote anahisi mzigo wa ombi, basi na aombe.


---

Baba yao alipokufa, ndugu za Yusufu walipata hofu gani? Yusufu alifanyeje? Yusufu alikufa akiwa na miaka mingapi? Aliwasihi watoto wake na wana wa Israeli wafanyeje kuhusu mifupa yake?

**SIKU YA 27**
**(Januari 27)**

# Kuzaliwa kwa Musa

**- Kutoka 1 na 2**



Kujisamehe mwenyewe ni jambo moja muhimu sana kwa afya, kama tulivyoona kwamba Yusufu aliwasamehe ila wao bado walishuku! Basi Wana wa Israeli (Yakobo) walizidi kuongezeka na kuwa wengi, wakaishi Misri miaka 430, wengi husema pengine ile miaka 30 walikuwa huru na 400 watumwa. Mwishowe akainuka Farao mpya kutawala asiyemjua Yusufu na kuwaambia watu wake, "Watu wa Israeli ni wengi, tena wana nguvu kuliko sisi. Haya! na tuwatendee kwa akili wasije wakaongezeka; tena, kukitokea vita wao nao wasije wakashikamana na adui zetu na kupigana nasi, na kutoka katika nchi hii". Wamisiri wakaweka wasimamizi juu ya Waisraeli ili wawatese kwa mizigo yao, nao wakamjengea Farao miji ya kuweka akiba huko Pithomu na Ramesesi.

Lakini kadiri walivyowatesa ndivyo walivyoongezeka na kuzidi kuenea. Wakawatumikisha kwa ukali na kufanya maisha yao kuwa machungu kwa kazi ngumu. Walifanya kazi ya chokaa, matofali, mashambani na zingine kwa ukali. Kisha Farao akawaambia wakunga wa Waebrania, Shifra na Pua kuwa wanapowazalisha wanawake wa Kiebrania, wakiona mtoto ni wa kiume wamwue papo hapo, ila mtoto wa kike aishi. Kwa vile mtoto wa kiume ndiye anachukua kabila, bali wa kike anapoolewa anakuwa taifa lile la mume wake. Wakunga hawa walikuwa wacha Mungu hivyo hawakufanya uovu ulioamriwa na mfalme, wakiwahifadhi hai watoto wa kiume. Mfalme Farao akawaita na kuwauliza ni kwa nini hawawaui watoto wa kiume? Walijibu, "wanawake wa Kiebrania si kama wanawake wa Ki-misri kwa kuwa ni hodari hao, nao huzaa kabla mzalishaji hajapata kuwafikia". Mungu akawabariki wakunga hawa akawatendea mema kwa kuwasimamishia nyumba zao. Farao akasema kila mtoto wa kiume azaliwaye atupwe mtoni, ila mwanamke ahifadhiwe. Huu ulikuwa ukatili wa ajabu. Japokuwa leo watu wengi si watumwa, huwa tunapata mateso ya namna nyingine. Basi sote tukumbuke ahadi

za Mungu kutuokoa kwenye mateso ya namna yo yote.

Hebu tusimame hapa na kufikiria huzuni ambayo wazazi waliipata wakati watoto wao wa kiume waliponyakuliwa kutoka kwao na kutupwa kwenye Mto Nile. Picha zenye kuhuzunisha tunazoziona leo kwenye runinga za watoto walio na utapiamlo na njaa katika nchi ambako vita vinaendelea zinaonyesha kwamba watoto bado wanapata mateso makubwa. Kwa kuongezea, kuna mamilioni ya watoto ambao hawajazaliwa ambao huuawa kwa njia ya utoaji mimba kila mwaka duniani kote, na picha inakuwa ya kutisha zaidi. tukiacha mbali na wale ambao wanaozaliwa lakini wanatendewa vibaya na watu wazima. Je, Mungu anajisikiaje akitazama haya yote? Hakika kuna adhabu ya kutisha inayowajia wale ambao wanawatendea watoto uovu. Bwana Yesu tafadhali uje upesi na uwaokoe watoto! Wakati huo huo, wale wanaowaleta watoto duniani wanapaswa kuwapa huduma bora zaidi, kwa maana watoto hawaombi wazaliwe. Wengine wamefiwa na wazazi wao wawili, na wamekuwa yatima, Je, nani atawatunza hawa? Wasamaria wema! Hebu Sote tuwe wasamaria wema.

Basi mtu mmoja wa nyumba ya Lawi aitwaye Amramu alioa mke aitwaye Yokebedi, na kuzaa mtoto ambaye jina lake lilipotea. Alimficha mtoto kwa miezi mitatu mpaka alipokuwa hawezi tena kumficha. Alimjengea kisafina cha nyasi na kukipaka sifa na lami, akamtia mtoto ndani yake na akaiweka kwenye majani kando ya mto. Nafikiri alilia machozi ya huzuni kumtupa mtoto. Miriamu, dada mkubwa wa mtoto, alikuwa na miaka sita, alikifuata kikapu ili ajue yatakayompata mdogo wake. Binti Farao akashuka aoge mtoni na vijakazi wake, naye akakiona kisafina kwenye majani, akamtuma mjakazi wake akilete. Akaona mtoto wa Kiebrania analia, naye akamhurumia. Miriamu kwa upendo kwa mdogo wake, alimwambia binti Farao, “Je, niende nikamwite mlezi katika wanawake wa Kiebrania aje kwako, akunyonyeshee mtoto huyu?” Binti Farao alikubali. Neema ya ajabu, mama yake Musa akaja na akamchukua mtoto kwake, akilipwa kumtumza mtoto wake kwa maadili ya kumcha Mungu, kisha akamrudisha. “Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha hata atakapokuwa mzee.” Hii ni ahadi ya Mungu. Pengine aliwaza atakaa naye muda gani akimtunzia ‘binti Farao.’ Akanuia kumfundisha Musa kumtumaini na kumtii Mungu, kwa sababu alijua ikulu ina fahari na anasa au majaribu mengi. Alimfundisha kuomba, kuimba na kisa cha uumbaji na kuanguka kwa mwanadamu. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao nyumbani au kuwapeleka shule ya kanisa miaka ya kwanza ya maisha yao kama wanataka kuleta tofauti katika maisha ya Kikristo. Kwa kiwango kikubwa sana mama anashikilia hatima ya watoto wake mikononi mwake. Kando ya Mungu Mwenyewe, hakuna aliye na ushawishi kwa mtoto kama mama.

Mama huyu hakuacha kumweleza mpango wa wokovu ambao walikuwa wameambiwa kwa vizazi vingi. Alimfundisha usafi wa moyo na Sheria Zake. Alimweleza ahadi alizopewa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Yokebedi akapata huzuni Musa alipokuja kuchukuliwa, pengine hata kaka Yake Haruni alipenda naye aende kuishi ikulu. Jina Musa lina maana “nilimtoa majini.” Alipewa hili jina na binti Farao. Musa aliyezaliwa mtumwa akawa mwana wa Farao! Wengi husema alienda baada ya kumaliza utoto yaani baada ya miaka 12, kwani waebrania mtoto wa miaka 13



ni mtu mzima kijana, anayefanyiwa sherehe muhimu inayoitwa 'bar mitzvah' Angalia video zake. Mungu ana mipango na maisha yako pia. Mama yake lazima alimweleza kisa cha kuokolewa kwake majini.

Musa akasoma elimu yote ya Misri kama mtoto wa Farao. Nafikiri alisomea Hesabu, mambo ya usalama/jeshi, uongozi, sheria ya nchi au hata utabibu. Alikuwa na uwezo na akafuzu mambo yote. Alipokuwa mtu mzima aliendа kuona ndugu zake Waebrania, hakutaka fahari ya kuitwa mwana wa Farao bali aliona ni bora apate mateso na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha kwa anasa za kitambo. Akaona Mungu ana thamani kuu kuliko hazina na utajiri wa Misri Alimwona Yeye asiyeonekana. Akatazama mateso yao na akamwona Mmisri anampiga Mwebrania. Alipotazama na kuona hakuna anayemwona, alimwua yule Mmisri, na kumzika kwa kificho. Kesho yake alikuja tena na tazama Waebrania wawili wanapigana, akamwambia yule aliyemdhulumu mwenzake, "mbona unampiga mwenzako?", naye akamjibu, "Ni nani amekuweka kuwa mwamuzi wetu? Je, unataka kuniua kama ulivyomwua yule Mmisri?" Alikuwa amezika mtu bali habari zilikuwa zimekwenda kote. Musa akaogopa akajua jambo lile limejulikana. Farao alipopata habari alitaka kumwua Musa, akiona analeta mapinduzi nchini. Musa akakimbia kwenda Midiani. Alifika Midiani, akaketi kwenye kisima. Musa hakuwa na uvumilivu wa kumngoja Mungu awaokoe Waisraeli. Akachukua sheria mikononi mwake, sasa alikuwa mtu asiye na mahali hata pa kulala. Tuache Mungu aongoze maisha yetu. Mungu anatuita kwa makusudi mbalimbali; hata hivyo mara nyingi tunajaribu kutatua changamoto sisi wenyewe na kufanya makosa ambayo yanaonekana kuwa hayawezi kurekebishwa. Hata hivyo, Mungu anaweza kutumia makosa yetu ili kutusaidia kukua. Mungu alitumia kosa la Musa huko Misri kumwongoza hadi nyikani ili ajifunze unyenyekevu na subira akiwa mchungaji. Huko akapata ujuzi unaohitajika wakati alipowaongoza Israeli jangwani. Musa hakuachwa kwa sababu alichafua. Mungu alitumia kutofaulu kwa Musa kumfundisha masomo yenye thamani ili kumtayarisha kwa ajili ya utume wake. Vivyo hivyo, Mungu ana kusudi kwa ajili yetu sote. Ingawa tunafanya makosa Mungu bado anaweza kututumia sisi na makosa yetu kwa utukufu Wake.

Yethro kuhani wa Midiani alikuwa na mabinti saba. Nao wakaenda kuteka maji ili kunywesha mifugo ya baba yao, wachungaji wengine wakawafukuza lakini Musa akasimama na kuwasaidia kunywesha kundi lao. Mabinti walirudi nyumbani, na baba yao aliwauliza kwamba imekuwaje wamerudi mapema. Wakaeleza kuwa Mmisri mmoja ametusaidia. Akawauliza mabinti zake, yuko wapi? Mbona mmemwacha, basi walienda wakamkaribisha Musa, naye akawa radhi kukaa nao. Yethro akampa binti yake aitwaye Sipora kuwa mkewe. Naye akamzalia mwana akamwita Gershomu, maana yake "nimekuwa mgeni katika nchi ya ugenini". Wamidiani ni wazao wa mke wa tatu wa Ibrahimu, yaani Ketura. Basi mfalme wa

Misri akafa na wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya utumwa, na kilio chao kikamfikia Mungu, Naye akakumbuka Agano Lake na Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Mateso yoyote yatukumbushe kwamba Mungu Yupo pamoja nasi kama vile ambavyo alivyokuwa pamoja na Masihi. Uwepo wa Mwenyezi Mungu daima ulimzunguka Kristo, na hakuna kilichompata isipokuwa kile upendo usio na kikomo ulichokiruhusu Kwake ili kuubariki ulimwengu. Hapa ndipo palikuwa chanzo Chake cha faraja, na kwa ajili yetu sisi pia. Yeye aliyejazwa Roho wa Kristo hukaa ndani ya Kristo. Pigo lolote linalolengwa kwake linamwangukia Mwokozi, anayemzunguka kwa uwepo Wake. Chochote kinachomjia kinatoka kwa Kristo. Yeye hana haja ya kupingana na uovu, kwa maana Kristo Ndiye ulinzi wake. Hakuna kinachoweza kumgusa isipokuwa kwa idhini ya Bwana wetu, na 'vitu vyote' vinaruhusiwa 'vifanye kazi pamoja kwa ajili ya mema kwa wale wanaompenda Mungu.' Warumi 8:28 . Hili linatuonyesha katika maisha yetu, lolote linalokuja, tumkabidhi Bwana, atupe nguvu, aondoe uchungu moyoni mwetu na kusamehe watesi wetu!

*Kuna wengine, nina hofu kwamba hawapeleki shida zao kwa MUNGU katika maombi ya faragha, lakini wanayahifadhi au kuyalimbikiza kwa ajili ya mkutano wa maombi, na hapo hufanya maombi yao kwa siku kadhaa. Watu hao wanaweza kuitwa wauaji wa mikutano na maombi (prayer and conference killers). Hawatoi nuru; hawamjengi mtu. Maombi yao ya baridi na marefu, yaliyoganda barafu na shuhuda zao ndefu, za kurudi kwao nyuma zinawekea watu kivuli. Wote wanafurahi wanapomaliza, na ni vigumu kuutupilia mbali ubaridi na giza ambalo maombi, hotuba au mawasiliano yao huleta kwenye mkutano. Kutoka katika nuru ambayo nimeipokea, mikutano yetu inapaswa kuwa ya kiroho na ya kijamii (kirafiki na mahusiano-social), na sio mirefu sana. Kukosa roho ya urafiki au kuwaweka watu mbali nawe, kiburi, ubatili, na hofu kwa mwanadamu vinapaswa kuachwa nyumbani. Tofauti ndogo na chuki haipaswi kwenda nasi kwenye mikutano hii. Kama ilivyo katika familia yenye umoja, usahili, unyenyekevu, upole, ujasiri, na upendo vinapaswa kuwepo mioyoni mwa akina kaka na dada ambao wanakutana ili kuburudishwa na kuongezewa nguvu kwa kuleta mianga yao pamoja.

---

Je, Waisraeli waliishi miaka mingapi Misri? Kwa nini Farao aliamuru kuua watoto wa kiume? Wakunga walitoa udhuru gani dhidi ya kuua watoto walipokuwa wakizaliwa? Maana ya Musa ni nini? Wazazi wa Musa ni nani? Dada ya Musa aliitwa nani? Kwa nini Musa alikimbia kutoka Misri? Yethro alikuwa na kazi gani? Mke wa Musa aliitwa nani? Biblia haina neno 'teenager' au kiswahili, ila mtoto akifika ujana, unafikiri ni mambo gani afundishwe?

**SIKU YA 28**
**(Januari 28)**

# Mateso Yawafanya Wawe Imara na Musa na Kijiti Kilichowaka Moto

**- Kutoka 3 na 4**



Mungu anaona kila chozi la waliovunjika moyo. Ikiwa inaonekana kwamba Mungu hachukui hatua haraka, hiyo haimaanishi kwamba Yeye hali zetu. Musa alikuwa mchungaji wa kundi la Yethro mkwewe, kuhani wa Midiani kwa miaka 40. Akiliongoza kundi la mifugo karibu na mlima wa Mungu, Horebu, Musa alikuwa amekuwa mpole, mnyenyekevu, na mvumlivu, ndipo, malaika wa Bwana akamtokea. Musa akaona mwali wa moto kwenye kichaka. Kichaka kiliendelea kuwaka moto, bali hakikuteketea. Mungu aliona kuwa mtu Wake Musa yupo tayari sasa kutumiwa Naye, kwa sababu alikuwa mnyenyekevu akijua kuwa ni Mungu Ndiye atawaokoa Waisraeli na si yeye. Mungu anapomwita mtu, humwezesha. Basi, Musa akawa na udadisi akasogea ili atazame kinachoendelea. Bwana Mungu akamwita, "Musa, Musa!" akajibu "Mimi hapa". Musa alikuwa na miaka 80 naye akaambiwa "usikaribie hapa, vua viatu miguuni mwako, maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu". Akamwambia "Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Ibrahimu, …. Isaka …. na Yakobo". Musa akaficha uso wake akiogopa kumwangalia Mungu. Mungu akamwambia ameyaona mateso na maumivu ya watu wake Waebrania walio Misri na kusikia kilio chao kwa wasimamizi wakatili, naye ameshuka awaokoe. Awapandishe katika nchi ile njema ya Kanaani, nchi ijaayo maziwa na asali, mahali pa Wakanaani, Wahiti, Waamori, Wahivi, Waperizi, na Wayebusi. Akamwambia ninakutuma kwa Farao ili upate kuwatoa watu wangu, hao wana wa Israeli kutoka Misri. Musa alikuwa tayari kwa utumishi, akiwa mtu mnyenyekevu, akijua ni Mungu tu Ndiye atakayewatoa utumwani na si yeye. Musa aliua mtu na kufanya dhambi, wakati Mungu Ndiye angemsaidia kuwaokoa Israeli na si yeye.

Baada ya miaka 40 ya kuchunga kondoo, na kisomo kikubwa, alikuwa amenyenyekea na Mungu akaona ni chombo kiteule cha kufaa sasa kufanya kazi yake. Akamwambia Mungu, "mimi ni nani hata niende nikawatoe wana wa Israeli watoke Misri?" Bwana akamwambia atakuwa naye, na akamwambia wakitoka watakuja kwenye mlima

wa Horebu kumwabudu Mungu. Naye Musa akasema Waisraeli wakimwuliza atakaposema kuwa “Mungu wa baba zenu amenituma kwenu” awaambie Jina Lake ni nani? Mungu akasema, “MIMI NIKO AMBAYE NIKO”. Waambie “MIMI NIKO” amenituma. Mungu akamwambia Musa, aseme “Mungu wa Baba zenu ... Ibrahimu ... Isaka ... Yakobo” amenituma na hili ndilo Jina Lake hata milele, nalo ni kumbukumbu ya vizazi vyote. MIMI NIKO maana yake ni uwepo wa milele; zamani, sasa, na wakati ujao. Anaona matukio ya mbali zaidi ya historia iliyopita na wakati ujao waziwazi maana ana uwezo wote. Musa akatuma akusanye wazee wa Israeli pamoja na kuwaambia “BWANA, Mungu wa Ibrahimu ... Isaka ... Yakobo amenitokea na akaniambia nitawajilieni tena, nimeyaona mnayotendewa huko Misri.” Naye Mungu atawapandisha kutoka katika mateso ya Misri na kuwaingiza katika nchi ya Kanaani ijaayo maziwa na asali.

Musa akaogopa akiona hawatamwamini wakisikia sauti yake, watasema “Bwana hakukutokea”. BWANA akamwuliza Musa ana nini mkononi? Musa akasema fimbo. BWANA akamwagiza aitupe chini, nayo ikawa nyoka. Bwana akamwambia Musa amshike nyoka mkia, na nyoka akageuka kuwa fimbo tena. Kisha BWANA akamwamuru aweke mkono wake kifuani, naye alipoutoa ukawa mweupe kama theluji kwa ukoma. Naye akaamriwa aurudishe kifuani na kuutoa, ukawa umerudia hali ya mwili wake. Alipewa hizi ishara mbili kuonyesha kwa Farao haamini. Akaambiwa wasipoamini basi yatwae maji ya mtoni na umwage nchi kavu na yale maji uyatwaayo mtoni yatakuwa damu juu ya nchi kavu. Musa akatoa udhuru “Ee BWANA mimi si msemaji, ... maana mimi si mwepesi wa kusema, na ulimi wangu ni mzito”. BWANA akamkumbusha “Ni nani aliyekifanya kinywa cha mwanadamu?... au ni nani afanyaye mtu kuwa bubu au kiziwi, au mwenye kuona, au kuwa kipofu, si Mimi BWANA?” BWANA akamsisitiza Musa aende, naye atakuwa pamoja na mdomo wake, na kumfundisha atakalolinena. Musa akazidi kuzungumza mashaka, Mungu akakasirika na kusema “Je, hayuko Haruni ndugu yako mlawi?” Yeye anaweza kusema vizuri na atakuja kukulaki, na atafurahi atakapokuona. Akamwambia Musa amwambie Haruni yote ambayo Mungu alimwagiza, “naye atakuwa msemaji wako kwa watu, na kuwa mfano wa kinywa kwako”. Akaambiwa aende na ile fimbo ili kufanya ishara.

Kitabu hiki kinatuambia, Mungu ANAONA kinachoendelea, ANASIKIA vilio, ANAJUA kuhusu tatizo, ANAJALI na ATASHUGHULIKIA. Jambo hili linanifarini na kunitia moyo katika ulimwengu huu uliovunjika tunamoishi, kwamba haijalishi ni nini kinaendelea, Mungu ana udhibiti kamili. Hata wakati Roho wa Mungu anaishi ndani yetu: Tutastukia tumo ndani ya mitihani mikali ambapo watu watatutazamia tuvunjike, lakini hakuna mtu atavunjika! Watatukodolea macho, nasi hatutaangamizwa. Kwani Si kwa uwezo wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho Wangu, asema Bwana wa majeshi. Zekaria 4:6 Mtu fulani alisema, Musa alishindwa kumzika Mmisri mmoja tu ambaye alimuua, lakini Mungu aliweza kulizika jeshi lote la Wamisri katika Bahari ya Shamu!

Musa akaenda kwa baba mkwe wake Yethro na kuomba ruhusa awarudie ndugu zake waliokuwa Misri, ili aone kama wako hai. Yethro (Reueli) akakubali, “Nenda kwa amani”. Mungu akamwambia wale wote waliotaka kumwua kule Misri

wamekwisha kufa. Musa akamchukua Mkewe na wanawe wawili akaenda Misri na ile fimbo mkononi. BWANA akamwambia afanye zile ishara za ajabu mbele ya Farao, lakini Farao ataufanya moyo wake kuwa mgumu, naye hatatoa ruhusu kirahisi. Mungu akamwambia Musa amwambie Farao "Israeli ni mwanangu Mimi, mzaliwa wa kwanza Wangu, Nami nimekuambia, mpe mwanangu ruhusa aende, ili apate kunitumikia, nawe umekataa kumpa ruhusa … angalia … Mimi nitamwua mwanao, mzaliwa kwa kwanza wako". Musa akaanza safari na akiwa njiani, BWANA akakutana naye akataka amwue Musa kwa kutokumtahiri mwana wake wa kwanza, ndipo Sipora akamtahiri mtoto haraka na jiwe na kuzuia ile adhabu. Hata tukiwa tunamfanyia kazi Mungu, bado tunapaswa kutii mambo madogo na makubwa. Musa alikuwa kuhani na kiongozi wa nyumba yake, japo alijulikana kama shujaa, na Mungu alikuwa amemtayarisha kwa miaka mingi, alikuwa ni mtumishi tu na alipaswa kutii. Mungu alitaka kumwua kama ambavyo alikuwa amemwua mwana wa kwanza wa Farao punde tu kwa kutotii! Yawezekana mke wake ndiye alikuwa msaada na kuchukua jukumu kama kisa kinavyosema au yawezekana alikuwa akipinga kutokana na kisa kwasababu hakuwa myahudi. Hili ni somo kwa wanandoa wote wasiutweze utume ambao Mungu amewapa wenzi wao na pia kwa watu wanaoshika nyadhifa kubwa, kwamba tunahitaji kutii zaidi hata kuliko wengine. Musa alikuwa anaenda kuchukua nyadhifa yenye hatari kubwa; uhai wake ungeweza kuhifadhiwa tu kupitia ulinzi wa malaika watakatifu. Lakini wakati anapuuzia wajibu unaojulikana, hangekuwa salama; kwani hangeweza kulindwa na malaika wa Mungu.

Mungu akamwambia Haruni wakutane na mdogo wake penye Mlima wa Mungu, yaani, mlima Horebu. Kaka wawili wakafurahiana baada ya miaka 40. Musa akiwa na miaka 80 na Haruni miaka 83. Musa akamwambia kaka yake Maagizo aliyopewa na BWANA na ishara alizomwagiza. Haruni na Musa wakaenda na kukusanya wazee wa Israeli, nao wakafanya zile ishara na watu wakaamini ya kuwa Mungu amewajilia Waisraeli na ameona mateso yao, wakainamisha vichwa vyao na kusujudu. Haruni alikuwa amemwoa Eliseba na kupata wana wanne nao ni Nadabu, Abihu, Eleazari na Ithamari. Inasemekana Miriamu alikuwa ameolewa na Huri.

Ingawa Waisraeli walikuwa wamekaa Misri kwa zaidi ya miaka 400 na hawakujua tena majina ya familia zao, Mungu bado aliwajua kwa majina. Naye alikuwa akiwatayarisha kumsikia akitamka Jina Lake Mwenyewe (YHWH) kwa sauti ya kusikika vyema kule Sinai. Kwa Waebrania kitabu cha Kutoka ni injili: hadithi ya ukombozi, na neema. Kama Waisraeli na Musa, sisi pia tuliokolewa na Mtoto mchanga ambaye alikuwa Mkombozi. Karibu na mwisho wa maisha yake, Yesu alipanda mlima wa Kanaani na kukutana na Musa, pamoja na Eliya. Luka 9:31-32 husema kwamba walizungumzia "kuondoka" kwa Yesu—kihalisi, "kutoka" Kwake. Ni katika njia zipi kuhitaji kwa Waisraeli kukombolewa kunakukumbusha haliyetu sisi wenyewe? Je, unaweza kufikiria wakati ambapo "Farao mpya" aliinuka katika maisha yako na kufanya mambo kuwa magumu mno?

*Tumia Lugha Rahisi Unapoomba Hadharani—Lugha ya madoido mengi, misamiati mipya mingi, sauti ya juu yenye kujieleza sana na ya kutia chumvi haifai katika sala (highflown), iwe ombi hilo linatolewa mimbarani, katika mzunguko wa familia, au kwa siri. Hasa kwa yule anayetoa ombi la hadharani anapaswa kutumia lugha rahisi, ili wengine waelewe yanayosemwa na kuungana katika ombi hilo.

---

Taja vitabu vya Torati? Kwa nini Farao aliwaogopa Waisraeli? Je, kwa nini Musa alienda Midiani? Je, unafikiri Musa aliona kazi ya kuchunga ni rahisi? Kwa nini Mungu alimfanya Musa kuwa mchungaji? Je, moto alioona Musa ulikuwa na ajabu gani? Kwa nini alitoa viatu? Taja majina ya wana wa Haruni wanne? Mungu alimwambia Musa awape ishara gani Waisraeli ili wamwamini? MIMI NIKO ni nani?

**SIKU Ya 29**
**(Januari 29)**

# Musa Awezeshwa kuwa Mbele ya Farao

**- Kutoka 5-7**



Fimbo ya Musa ikawa fimbo ya Mungu. Una nini mkononi mwako leo? Tunaposalimisha vyote tulivyo navyo kwa BWANA, Yetu atafanya kazi ndani yetu na kama mawakala Wake, kwa njia za miujiza! Yeye huchagua mawakala Wake si kwa sababu wao ni wakamilifu bali kwa sababu, kupitia kuunganishwa kwao Naye, Yeye Mwenyewe atawakamilisha. Sisi pia ni vyombo mikononi mwa Mungu na pia wakati mwingine tunasahau kwamba hatuwezi kuwaokoa wanadamu kutoka mikononi mwa Shetani peke yetu. Hatuwezi kubadili tabia zilizokita mizizi, lakini Mungu kupitia Roho Wake anaweza kufanya hivyo. Anapotutuma kuhubiri injili hii ya ufalme Wake, anajua upinzani tunaoweza kukutana nao lakini kama alivyomuahidi Musa atatutendea makuu nasi. Sisi tu vyombo tu, Je, Mungu alimhitaji Musa kuwakomboa Waebrania kutoka Misri? Hapana. Je, Mungu anatuhitaji sisi kuwaweka watu huru kutoka kwa dhambini? Hapana. Ila Mungu anatuita tufanye kazi Naye kwa sababu anazozijua Yeye. Na Kabla Mungu hajatuambia tumwamini, Yeye hutupa ushahidi. Kwa hiyo imani yetu si ya kumangamanga tu gizani.

Basi Musa na Haruni wakaenda mbele ya Farao na kumwambia kuwa BWANA Mungu asema, “Wape ruhusa watu Wangu waende ili kunifanyia sikukuu jangwani”.

Farao akajibu kwa dharau akisema BWANA ni nani hata nisikilize sauti Yake na kuwapa ruhusa Waisraeli ruhusu waende zao, "simjui BWANA wala sitawapa ruhusa". Farao alikuwa ameshamjua Mungu wa Israeli kutoka na Historia ila ujeuri na kiburi kilimponza. Basi wakamwambia kuwa wamekutana na Mungu wa Waebrania na inabidi waende safari ya siku tatu jangwani na kumtolea dhabihu Mungu ili asije akawapiga kwa tauni au upanga. Farao akawaambia kwa nini wanawaachisha watu kazi. Farao akaamuru wanyapara wasiwape tena watu majani ya kutengenezea matofali bali waende kutafuta majani wao wenyewe na kutengeneza idadi ileile ya matofali maana ni wavivu na wanapiga kelele. Eti wanasema "tupe ruhusu twende kumtolea Mungu wetu dhabihu". Akafanya wapewe kazi nzito, wataabike "ili wasiangalie maneno ya uongo". Watu wakatawanyika wapate kukusanya majani na wanyapara wakawa wanatoa amri za shughuli za kila siku ziendelee kama wakati ambapo majani yalikuwapo. Wanyapara wakawapiga, na kuwaambia "kwa nini hamkumaliza kazi mliyopewa jana na leo?" Wanyapara, yaani wasimamizi, wakamlilia Farao, kwa nini anawafanyia vile, kwa kutowapa watumwa majani? Farao akasema ni wavivu tu. Farao akawaambia waendelee na kazi na hawatapewa majani; wanyapara wakaona hali ni mbaya na wakakutana na Musa na Haruni wakawalalamikia. Wakasema maisha yao yalikuwa na nafuu mpaka yeye na Haruni walipoenda kwa Farao kumwambia awaruhusu kwenda kutoa dhabihu kwa Mungu wao. "Mmetia harufu yetu kuwa chukizo mbele ya Farao na watumwa wake…watuue".

BWANA akamwambia Musa 'sasa utaona nitakavyomtenda Farao" naye atawapa ruhusa kwenda na kwa mkono hodari wa Mungu atawafukuza katika nchi yake. Mungu akamwambia Musa "MIMI NI YEHOVA" niliyemtokea Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Nimelithibitisha agano langu nao na kuwapa nchi ya Kanaani. Akamkumbusha kuwa amesikia kilio chao, na akalikumbuka Agano Lake, Naye ni "YEHOVA" Naye atawatoa chini ya mzigo wa Wamisri. Nao watakuwa watu Wake, Naye atakuwa Mungu wao, kwani atawakomboa kwa mkono ulionyoshwa na kwa hukumu kubwa. Kuna miungu mingi duniani ambayo siyo ya Kweli. Inasemekana nchi kama India ina miungu zaidi ya milioni 600. Ukiwa na shida ya kujua Mungu wa Kweli aliyeumba mbingu na nchi, kumbuka ni Mungu wa Ibrahimu, na Isaka na Yakobo. Ndiye pekee Mungu wa Kweli. Mahali pengine mtu amechukua mti na kipande chake, amechonga na kukifanya kama mungu na kukiabudu, na kipande anatengeneza kiti cha kukalia, na kipande anatumia kama kuni kupikia chakula. Mungu wa Kweli ni Mungu Aliye hai. Soma kuhusu Mungu Huyu na umfuate, Ndiye Mungu pekee Aliye hai, anayetawala, Ndiye Mwanzo na Mwisho, Alfa na Omega au Mfalme wa wafalme.

BWANA akamwambia tena Musa azungumze na Farao ili awape ruhusu watoke katika nchi yake. Naye Musa akasema kwa BWANA wana wa Israeli tu hawajanisikiliza, je, Farao atanisikiliza, niliye na midomo isiyo na tohara? Musa aligundua hekima ya kukaa kimya na kuacha Mungu ampiganie! Mungu anataka kuwa Mungu wetu, si tu Mungu wa baba na mama zetu, au wachungaji wetu. Anataka kuwa Mkombozi wetu. Je, tutaondoa macho yetu kutokana na mashaka yetu? Je, tutainua vichwa vyetu na kuweka tumaini letu kwa Yule ambaye anatamani kutusaidia na ukombozi ambao tayari ametimiza kwa niaba yetu? Tunapoteswa na kupata dhiki tukumbuke

na kudai ahadi za Mungu za ukombozi. Ijapokuwa ahadi imechelewa kwa muda mrefu, Yesu atatimiza ahadi Yake ya kuja tena ili kutuchukua mbinguni (Yohana 14:1-3), kwa maana ni rahisi zaidi kwa mbingu na dunia kutoweka kuliko Neno Lake lisitimie! Haidhuru Shetani atafanya nini ili kulizuia hili, Mungu atawachukua watu Wake hadi Kanaani ya mbinguni!

BWANA akamwambia Musa kwamba amemfanya yeye kuwa kama Mungu kwa Farao na huyo ndugu yake Haruni atakuwa nabii wake, na Musa anene Yale Mungu atakayomwagiza na Haruni atanena na Farao ili awape wana wa Israeli ruhusa watoke nchini kwake. Akasema tena ataufanya moyo wa Farao kuwa mgumu, na atafanya ishara nyingi za ajabu katika nchi ya Misri. Ugumu wa moyo wa Farao ulikuja kwa vile Roho wa Mungu alimtoka na akakosa ushauri wa Mungu, na hivyo akaendelea na uasi pasipo kuacha. Musa akaona hajasikia bado, wala hajamjua Mungu bado kwamba Ndiye BWANA. Musa akayapiga maji ya mto nayo yakawa damu". Basi maji yote ya Misri yakawa damu na samaki wakafa na mto ukatoa uvundo. Wamisiri wakachukia kunywa maji ya uvundo baada ya Haruni kushika fimbo na kunyosha juu ya maji na mito/vijito vyote vya Misri. Maji katika vyombo vyote vyenye maji, vya miti na mawe, yakawa damu pia. Waganga wa Misri wakaigiza hili pia, na moyo wa Farao ukawa mgumu, wala hakuwasikiza kama BWANA alivyonena. Farao akaendelea na shughuli zake akizunguka kwenda kwake bila kutilia maanani. Wamisri walichimba maji ya kunywa kando ya mto, kwa siku saba baada ya Bwana kuupiga mto.

Baada ya hili pigo, BWANA akamwamuru Musa aende kwa Farao tena. Mungu akitupatia kazi ya kufanya, mara zote anatoa uwezo wa kuifanya na kuleta majibu kwa matatizo yetu. Hebu hii itupe ujasiri wa kusonga mbele! Tukiwa Waaminifu kwa Mungu, Yeye atatutumia katika utoto hadi uzee wetu.

*Mungu Anapaswa kukaribiwa kwa kicho Katika Sala— Wengine hufikiri kuwa ni alama ya unyenyekevu kusali kwa MUNGU kwa njia ya mazoea au ya kawaida, kama vile wanavyozungumza na mwanadamu wenzao. Wanalichafua Jina Lake kwa kuchanganya pamoja bila ulazima na bila kicho sala zao maneno, "MUNGU Mwenyezi," Maneno matakatifu ya kutisha, ambayo hayapaswi kamwe kutoka midomoni mwao isipokuwa kwa sauti iliyotiishwa na kwa hisia ya kicho, inayohisi utukufu na utakatifu wa Mungu.

---

Kwa nini wanyapara walimlalamikia Musa? Kwa nini Moyo wa Farao ulikuwa mgumu? Waganga wa Misri waliwezaje kuigiza miujiza? Pigo la kwanza lilikuwa nini? Kuna tofauti gani kati ya Mungu na miungu?

**SIKU YA 30**
**(Januari 30)**

# Mapigo ya Misri

**- Kutoka 8-11**



Basi Musa akaenda kwa Farao tena na kumwambia "BWANA asema …. wape watu wangu ruhusa ili wapate kunitumikia". Musa akamwambia Farao kuwa kama akikataa, basi vyura wataletwa. Farao alikataa, na Musa kwa Amri ya Bwana alinyosha mkono juu ya mito na vijito na maziwa na vyura wakatokea wengi na wakaingia ndani ya vyumba vya kulala, vitandani, na kwenye vyombo vya kulia. Vyura wakaifunika nchi, na waganga wakaweza kuigiza kuleta vyura juu ya nchi. Farao alichoka na vyura kila mahali na akamwomba Musa amwambie BWANA awaondoe. Musa akamwuliza anataka jambo hili lifanyike lini? Farao alijibu kuwa iwe kesho yake. Musa alimlilia BWANA Naye BWANA akafanya vile Musa alivyomwahidi Farao kwa imani. Vyura walikufa viwanjani na mashambani na watu waliwakusanya, na kwa sababu ya kuoza nchi ilitoa uvundo.

Farao alipoona unafuu akaufanya moyo wake kuwa mzito asiwasikize kama BWANA alivyonena. Musa akanyosha tena fimbo yake akayapiga mavumbi ya nchi, yakawa chawa. Kila mtu na wanyama wakawa na chawa wengi, hata Farao na watumishi wake. Waganga walijaribu kuigiza kuleta chawa wasiweze, wakamweleza Farao kwamba "jambo hili ni chanda cha Mungu". Moyo wa Farao ukawa mgumu asiweze kuwasikiliza. Binadamu wengi tukiwa tuna tatizo kubwa tuko tayari kusikia sauti ya Mungu, ila Mungu akitusaidia tunajisahau, hili litufanye macho yetu yafunguke!

Asubuhi walimfuata Farao aliyekuwa majini, awape ruhusa Waisraeli waondoke, lakini alikataa na pigo la mainzi likaletwa. Pigo hili lilikuwa kwa Wamisri tu. Inzi walikuwa wengi mno. Farao akawaambia wana wa Israeli waende wakamtolee

kafara Mungu wao lakini wasiende mbali. Musa alisema wanataka kumchinjia Mungu dhabihu na hii ni machukizo kwa Wamisri hivyo lazima wafanye safari ya siku tatu jangwani. Musa alitoa mainzi hawa bali Farao alifanya moyo wake mgumu kuwapa ruhusa Waisraeli waende. Baada ya Farao kupata adhabu zote hizi, hakuacha uovu na kutosikia sauti ya Mungu. Basi mifugo yake kama farasi, punda, ngamia, ng'ombe na kondoo walipata tauni ya majipu ya kufura na kutumbuka baada ya Musa kurusha majivu kuelekea mbinguni mbele ya Farao; bali wanyama wa Waisraeli Bwana aliwatenga na hivyo hawakufa. Hata waganga walishindwa kuja tena kwa Farao kwa kushikwa na majipu. Baada ya hapo likaja pigo la mvua ya mawe nzito sana, na Farao aliambiwa ajitayarishe kwa kuweka wanyama wake salama. Tufani nzito ya ngurumo ilikuja na kuvunja miti, mazao ya mashambani na vitu vyote. Farao akamwambia Musa kuwa, yeye na watu wake ni waovu na wamekosa, na BWANA ni Mwenye haki. Basi BWANA alipokomesha tufani, Farao aliendelea kuwa na moyo mzito, na hata BWANA akauliza "utakataa hata lini kujinyenyekeza mbele Zangu? Wape watu Wangu ruhusa waende zao ili wanitumikie".

Basi pigo la nane la nzige likaletwa nao wakafunika uso wa nchi. Nzige wakala kila kitu mashambani kilichosalia wakati wa mvua ya mawe. Jambo la ajabu ni kuwa, hata baada ya mapigo haya, bado Farao alifanya kiburi asibadilike na kusikia sauti ya Mungu. Hata leo, ukaidi unatokea kwa binadamu pia. Basi Farao aliwaambia, "waende watu wazima tu kutoa kafara, bali waache watoto wao". Farao alisihi Mungu amsamehe, na "aniondolee kifo hiki tu". Musa alitoka na kumwomba Mungu, na BWANA akaugeuza upepo na kuwaondoa wale nzige. Basi Farao akawa na moyo mgumu, na pigo la tisa la giza zito kwa siku tatu likaja kwa Wamisri. Kuwa na moyo mgumu ni jambo la kumletea mtu matatizo makubwa. Giza lilikuwa nene sana hata hawakuweza kuonana. Farao akawaambia waende kumtumikia BWANA lakini bila mifugo yao. Musa akasema walihitaji mifugo ili kutoa kafara kwa BWANA. Farao alikasirika na kumfukuza Musa akisema, "Nenda zako, usinione uso tena". Musa akasema sawa umenena vyema sitakuangalia uso wako tena, ikawa mwisho wa kwenda kwa Farao. BWANA akaleta pigo la mwisho la kumi la kufa kwa mzaliwa wa kwanza wa binadamu na hata wanyama. Akawaambia kwamba mwana wa kwanza wa Farao atakapokufa, atawapa ninyi ruhusa mtoke kabisa katika Misri. Musa akapewa maagizo na BWANA kuwaambia wana wa Israeli waende kwa jirani zao na kuomba vyombo vya fedha na dhahabu, naye BWANA akawapa kibali machoni pa Wamisri kutoa vitu vyao kirahisi. BWANA akamwambia Musa kwamba usiku wa manane atapita Misri na kuwapiga wazaliwa wa kwanza, kuanzia kijakazi mpaka kwenye ikulu ya Farao. Ila kwa Waisraeli hapana hata mbwa atakayetoa ulimi na hivyo watapata kujua jinsi BWANA alivyowatenga na Wamisri.

Kwa kila muujiza ambayo Musa na Haruni walifanya mbele ya Farao, wachawi wake waliweza kughushi tukio kama hilo (miujiza feki). Ushindani huu katika nyua ya Farao inatukumbusha Pambano Kuu kati ya wema na ubaya. Shetani anaweza kutumia uwezo wake mdogo kuleta mateso na huzuni kwenye sayari yetu, lakini hawezi kushindana na Muumba wa mbingu na dunia. Siku inakuja upesi ambapo kila goti litapigwa na kila ndimi itakiri kwamba Yesu Kristo ni BWANA kwa utukufu wa Mungu Baba. Kisha Pambano Kuu litakuwa limekwisha na kwa mara nyingine

tena ulimwengu utapata amani kamilifu. Ukweli unabaki pale pale kwamba nguvu ambazo Mungu alimpa Shetani wakati anaumbwa hazijaondolewa (kama Mungu angemnyang'anya uwezo wake, angedai kuwa ndiyo sababu ya kutoweza kutoa maisha bora kuliko yale ambayo Mungu anaweza kutoa kwetu). Hakika anao uwezo fulani wa kuwawezesha mawakala wake wa kibinadamu kufanya miujiza. Kwa hiyo Bwana wetu Yesu anatuonya, katika muktadha wa matukio ya siku za mwisho: "Kwa maana watatokea wakristo wa uongo na manabii wa uongo na kuonyesha ishara kubwa na maajabu ili kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule" Mt. 24:24. Njia pekee ya kuepuka kudanganywa ni kwenda daima kwenye Neno la Mungu: "Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi." Isa. 8:20 .

*Ni Fursa Yetu Kupiga Magoti Tunapoomba Hadharani—Katika ibada ya hadhara na faraghani ni wajibu wetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotoa maombi yetu Kwake. Tendo hili linaonyesha utegemezi wetu kwa MUNGU.

---

Ni mapigo mangapi yalikuwa kwa Wamisri tu? Kwa nini wachawi walishindwa kuigiza mapigo? Pigo la mwisho lilikuwa lipi? Kwa nini Farao hakutaka kuwaachilia Waisraeli? Ufunuo 16 inaeleza mapigo haya yanakuja siku za karibuni kabla ya dunia kwisha, Je tujitayarisheje na haya mapigo?

**SIKU YA 31**
**(Januari 31)**

# Pasaka ya Kwanza

**- Kutoka 12 na 13**

BWANA akamwambia Musa "Mwezi huu utakuwa mwezi wa kwanza wa mwaka kwenu". Wakaamrishwa kutwaa kondoo kwa hesabu ya kila nyumba na ikiwa ni wachache wajiunge na majirani na kutwaa mwanakondoo au mwanambuzi mmoja asiye na hila (kilema) kadiri ya ulaji wao. Watoto na watu wazima walianza kufurahia kwani ilibakia muda mchache tu wangetoka utumwani, na ndiyo maana kitabu cha pili katika Biblia kinaitwa "Kutoka", yaani kutoka Misri. Siku ya kumi wangemtwaa huyu mwanakondoo na kumchinja jioni, na kutwaa baadhi ya damu yake na kuitia katika miimo miwili na katika kizingiti cha juu cha milango ya nyumba zao. Waliamriwa kula nyama yake usiku ule ule, iliyookwa motoni, pamoja na mkate usiotiwa chachu na mboga chungu zikiashiria uchungu wa utumwa. Waliambiwa waoke vizuri sehemu zake zote na kula bila kusaza. Ikiwa kitabakia cho chote mpaka asubuhi, walitakiwa wakichome kwa moto. Waliambiwa kula huku wamejifunga viuno vyao, na kuvaa viatu vyao wakiwa tayari na fimbo zao zikiwa mikononi na kula kwa haraka, kwani ni pasaka ya BWANA.



Usiku ule Bwana angepita katika nchi ya Misri na kuwapiga wazaliwa wa kwanza wa wanyama na wanadamu na kufanya hukumu juu ya miungu yote ya Misri. Damu ilikuwa ni ishara ya agano katika zile nyumba ambazo (atazipita) ataziruka na kutopatwa na pigo la mauti. Siku hiyo ikawa ukumbusho na sikukuu ambayo hata Wayahudi wanaiadhimisha mpaka leo. Wakaambiwa kuwa katika sikukuu hiyo watakuwa wanakula mikate isiyochachwa kwa siku saba, na ye yote atakayekiuka agizo hilo angekatiliwa mbali na Israeli. Siku ya kwanza na ya nane zingekuwa kusanyiko takatifu, na kazi zozote zisingefanyika isipokuwa zile zilizohusiana na Pasaka. Siku hii ilitolewa waitunze kama sikukuu ya mikate isiyochacha ili kukumbuka Mungu alivyowatoa Misri. Huu ulikuwa mwezi wa kwanza, siku ya kumi na nne, na wakala wakati wa jioni wakitii maagizo ya Mungu yaliyopitia kwa nabii Musa. Na hiyo ikawa ndiyo mwanzo wa mwaka wa Waisraeli. Hata leo, Mungu anashughulika kututoa katika utumwa mwa dhambi. Kama tukikubali, atatutoa katika utumwa wa dhambi. Wamisri waliotii maagizo haya walipata wokovu, ila Waisraeli waliopuuzia walifiwa na wana wao wa kwanza. Haijalishi u wa kabila, rangi au lugha gani, unapoamua

kumtii Mungu, baraka Zake zitaandamana nawe. Hivyo ndivyo afanyavyo kazi. Chagua kumsikiliza Mungu, hasa unapohisi unawasababishia wengine maumivu. Mara nyingi sisi ni Mafarao wetu wenyewe, kwa hivyo kabla hatujamkosoa yule aliye katika kisa hiki, hebu tujiangalie ndani yetu. Inaweza kuwa dhana fulani ya kisayansi, au falsafa potofu, au uraibu fulani unaodhoofisha ambao tumeingia. Hebu tujifunze somo kutoka kwa Farao. Kiongozi anapofanya maamuzi mabaya kila mtu chini ya uongozi wake huumia. Watumishi walimsihi Farao awaruhusu watu waende la sivyo Misri itaharibika, na hakika iliharibika, na kisha wakapata msiba wa watoto wao wa kwanza. Je, unazuiwa na kitu ambacho unafikiri ni muhimu zaidi kuliko wewe kumfuata Mungu kikamilifu?

Hata ikawa usiku wa manane, BWANA akawapiga wazaliwa kwa kwanza wa Farao na watu wote wa Misri, pakawa na kilio kikuu, maana hapakuwa na nyumba hata moja asimokufa mtu. Farao aliwaita Musa na Haruni na kuwaambia waondoke kwake, waende kumtumikia Mungu wao na mifugo yao, pia akasema, "mkanibariki mimi pia". Wamisiri wakawahimiza watoke kwa haraka maana waliogopa kufa. Waisraeli walichukua vyombo vyao na vitu vyao wakaondoka. Kwa hesabu, walikuwa wanaume laki sita waliotoka Misri nao wakasafiri kutoka Ramesesi mpaka Sukothi. Wanaume hawa ni wale wa kuanzia umri wa miaka ishirini kwenda juu. Hatujui idadi kamili ya wanawake na watoto. Lilikuwa kundi kubwa pamoja na wanyama wao. Usiku huo ni kumbukumbu muhimu ya BWANA kuwatoa Misri, na pia kwetu sote binadamu, kwani BWANA ametutoa katika utumwa wa dhambi. Pengine hawakulala wakifurahia kuondoka usiku ule kwenda kwao. "Nakumbuka tuliposoma shule ya bweni Kifungilo, Lushoto. Ni mfano hafifu kwamba tulipofunga shule tulifurahi tulipoona mabasi yanakuja kutuchukua kwenda nyumbani! Tuliimba kwa furaha, kwenda nyumbani".

Maelfu ya kondoo wa pasaka waliochinjwa walimwakilisha Kristo, Mwana-Kondoo wa Mungu ambaye angechinjwa kama pasaka na kuchukua dhambi za ulimwengu. Wamisri wengine walitoroka mabwana zao siku ile na kufuatana na Waisraeli, Wengine waliona matendo makuu wakajiunga nao, hawa waliojichanganya walileta shida nyingi baadaye.

Kisha BWANA akamwambia Musa kwamba wazaliwa wote wa kwanza watakaswe na kuwekwa wakfu kuwa wa BWANA. Akawakumbusha walivyotoka nchi ya Misri mwezi wa Abibu. Na kwamba atakapowaleta nchi ya Wakaanani Wahiti, Waamori, Wahivi na Wayebusi nchi ya maziwa na asali aliyowaapia Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, waendelee kuitunza sikukuu hii. Wale ambao hawakutii waliangamiza watoto wao kama ilivyokuwa kwa Wamisri. Utii ni jambo la muhimu, Mungu akisema tunapaswa kusikia sauti Yake na kutii.

Basi taifa jipya lilizaliwa siku hiyo. Inachukua wiki mbili kutoka Misri mpaka Kaanani. Musa aliona msafara wa watu, hata naye akashangaa watafikaje wote hawa Kanaani? Akiongozwa na Mungu, hapa alianza kutumia uzoefu wake wa utawala. Wengine wasio Wayahudi pia walifuatana nao. Hawa baadaye walileta matatizo mengi ya kunungunika, pengine hata Musa alijisemea, "ningejua nigewakataza wasije". Wakaona Mapiramidi yanaendelea kupotea machoni pao.

Walitembea kwa mwendo wa kadiri kwa sababu ya mifugo na watoto, pia walichukua mifupa ya Yusufu kama walivyoahidi. Wakaenda Sukothi kisha wakapiga kambi Ethamu mpakani mwa jangwa ambayo ni kama kilometa 400 hivi kufika Kanaani. Waliongozwa na wingu mchana lililowakinga jua la jangwani, na usiku waliongozwa na nguzo ya moto, iliyowakinga na baridi. Uwepo wa Mungu ulikuwepo wakati wote. Mungu aliwaelekeza njia watakayoifuata, pengine akiwaepusha kupita katika nchi ya Wafilisti ili kuepuka vita. Japo wengi walikuwa hawaelewi kwa nini wachukue njia hiyo. Watu hawa walikuwa wamekaa utumwani, na hawakuwa na uwezo wa kupigana vita. Wakafika na kuweka kambi mahali palipoitwa Pihahirothi. Ikawa kama wanaelekea Ethiopia hivi. Wakawa wametoka kabisa Misri. Kitabu cha Kutoka kimeitwa hivyo kwa sababu walitoka Misri kuelekea Kanaani.
Mungu azidishe upendo wetu Kwake tunapotembea Naye, na kutumia saa moja ya kutafakari kila siku maisha ya Yesu. Vyura, chawa na nzi, Baba, tafadhali uwaondoe hao katika maisha yangu ya kiroho na usaidie moyo wangu kuwa mnyenyekevu, wa kufundishika na kujisalimisha kwa mapenzi yako. Farao alikuwa na kutubu feki, akasema nitawapa ruhusa mwende, mkamchinjie Bwana, Mungu wenu jangwani; lakini msiende mbali sana; niombeeni mimi. Makubaliano haya hayakufanywa kwa moyo uliokuwa tayari kuwaacha Waisraeli waende zao, bali alikuwa akipanga njia za kuwarudisha. Alisema nendeni lakini si mbali sana kwa sababu alijua kuwa pengine wana wa Israeli watakumbuka vyakula, na mengine ya Misri, Shetani hana shida na sisi tukiwa wakristo, kama hatutaacha uovu na kutakasa miili yetu, na kufuata Amri zake. Muumini asiye na imani, ni rahisi kujaribiwa na kurudi kwenye maisha ya awali. Tunahitaji kujisalimisha kabisa. Kitu kingine ambacho kilinigusa ni toba ya uwongo ya Farao. Farao alikiri kwamba alikuwa ametenda dhambi, kwamba "BWANA ni Mwenye haki" na angewaacha Waisraeli waende huru. Lakini ngurumo na mvua ya mawe zilipokoma, aliufanya moyo wake kuwa mgumu tena, wala hakuwaruhusu Waisraeli waende zao .Ni mara ngapi mimi hutenda kama Farao? Je, ni mara ngapi mimi humgeukia Mungu ili tu "kutoka katika taabu," wakati ninapaswa kuzingatia wema Wake? Wema Wake ndio kitu pekee kinachotuongoza kwenye toba ya kweli (Warumi 2:4).

*Hadharani na katika ibada binafsi ni fursa yetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotuma maombi yetu. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Luka 22:41. Juu ya wanafunzi Wake imeandikwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Matendo 9:40. Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Waefeso 3:14. Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Tazama Ezra 9: 5. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, na akashukuru mbele za MUNGU wake." Danieli 6:10.

---------------------------------------------

Wingu mchana na nguzo ya moto usiku zilikuwa kwa ajili ya nini? Pasaka ya kwanza ilisherehekewaje? Nini kilitokea kwa yule asiyeweka damu kwenye mwimo wa mlango? Waisraeli wanaume waliotoka Misri walikuwa wangapi? Waisraeli walipata vitu wapi? Ni taifa gani lilizaliwa siku ya kutoka Misri?

**SIKU YA 32**
**( Februari 1)**

# Kuvuka Bahari ya Shamu

**- Kutoka 14**



Wakiwa hapo Pihahirothi moyo wa Farao ukawa mgumu, naye akaamua kuwafuata ili awarudishe aliposikia wamekwisha kukimbia na wako jangwani. Wafanyakazi wake wasiolipwa mshahara walikuwa wanatokomea! Mungu akajipatia utukufu kwa Farao na jeshi lake lote na Wamisri wakajua kuwa Mungu Ndiye BWANA. Wamisri walisema, "Nini jambo hili ulilotenda kwa kuwaacha Waisraeli waende zao wasitutumikie". Farao akaandaa magari 600 ya farasi na wapanda farasi, akawafuata Waisraeli. Kila aliyeweza kupanda farasi wa jeshi alikwenda kuwafuata. Waisraeli walipoangalia na kuona Wamisri wanakuja nyuma yao, waliogopa sana na wakamlilia Bwana na wakamwambia Musa, "Je, hapakuwa na makaburi katika Misri ndio maana umetutoa huko ili tufe jangwani? Wakasema walimwambia toka zamani awaache wawatumikie Wamisri, kuliko kufia jangwani. Musa akajibu, "Msiogope simameni tu, mkauone wokovu wa BWANA atakaowafanyia leo; kwa maana hao Wamisri mliowaona leo hamtawaona tena milele. BWANA atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya". Watu walimlilia Musa. Naye akamlilia BWANA. BWANA akawambia Musa, "mbona unanililia mimi? Waambie wana wa Israeli waendelee mbele. Nawe inua fimbo yako ukanyoshe

mkono wako juu ya bahari na kuigawanya, nao wana wa Israeli watapita kati ya baharí katika nchi kavu". Basi Musa akatii Maagizo, na Bwana na aliponyosha mkono, akaifanya bahari irudi nyuma kwa upepo wa nguvu kutoka mashariki usiku kucha, akafanyiza njia baharini. Kama watu zaidi ya milioni tatu na mifugo ilivuka usiku ule, kwa mahesabu ya kukadiria, zilikuwa maili tatu za njia kavu ili wapite wote. Mungu anajali na kuwalinda watu wake. Basi wale Wamisri wakawa kama wamepigwa bumbuwazi, ila BWANA aliifanya mioyo yao kuwa migumu na wakaingia kuwafuatia wana wa Israeli. Walipoona Waisraeli wamepita nao wakaanza kufuatia ndani ya bahari. Farasi wote wa Farao na magari yake na wapanda Farasi. Ilikuwa imefika alfajiri. BWANA akawachungulia Wamisri na kufadhaisha jeshi lao. Akayaondoa magudurumu ya magari yao, hata yakaenda kwa uzito, na Wamisiri wakasema tukimbie mbele ya Israeli kwa kuwa BWANA anawapigania kinyume chetu.

Basi bahari ya shamu iliyofunguka wakati Malaika wa Mungu amekaa nyuma yao pale nguzo ilipokuwa, ilianza kurudi kwa nguvu Zake wakati Musa aliponyosha tena mkono wake juu ya bahari kwa amri ya Mungu kulipopambazuka. Wamisri wakakimbia mbele Yake lakini 'wakafagiliwa' na maji baharini, wakafunikwa, wanajeshi, magari na farasi pia, hakusalia hata mtu mmoja. Bali wana wa Israeli walienda salama. Soma Zaburi 136:15, je, umeelewa nini kwenye fungu hili? Ndivyo BWANA alivyowaokoa Israeli siku ile mikononi mwa Wamisri. Mungu akishaweka ahadi, ataitimiza. Tumeahidiwa kufika! Israeli ikaona kazi kubwa aliyoifanya BWANA juu ya Wamisri, wakamcha BWANA na kumwamini, na kumheshimu mtumishi Wake Musa. Ndipo Musa na wana wa Israeli wakamwimbia BWANA wakimtukuza, "Nitamwimbia BWANA, kwa maana ametukuka sana; farasi na mpanda farasi amewatupa baharini. BWANA ni nguvu zangu na wimbo wangu, Naye amekuwa wokovu wangu. Yeye ni Mungu wangu nami nitamsifu. Ni Mungu wa baba yangu nami nitamtukuza. BWANA ni Mungu wa vita. BWANA ndilo Jina Lake.....". Waweza kuendelea kusoma wimbo huu wa Musa. Nabii Miriamu, dada yake Musa, mwimbaji, naye aliitikia na matari akiongoza wanawake wa Israeli, "Mwimbieni BWANA kwa maana ametukuka sana, Farasi na mpanda Farasi amewatupa baharini". Ni jambo jema kumshukuru na kumsifu BWANA. BWANA hupendezwa na sifa za watu Wake. Anapotufanyia makubwa na mema mengi, tusisahau kutoa fadhila na shukurani. Kuvuka watu takribani milioni tatu kwa usiku mmoja tu, na mifugo yao, ni mwujiza. Acheni Mungu aitwe Mungu. Kwani hakikuwa kinjia bali barabara pana, na kavu kabisa, bila majimaji. Watu wengi wamesema idadi hiyo ya watu kupita kwenye bahari ya Shamu (Red Sea) kule kwenye Suez Canal iliyojengwa mwaka 1869. Kuvuka kwenye upana wake ni kama Km 350 hivi, Na kina chake kama Km mbili hivi.

Mtu mmoja asiyemwamini Mungu aliwaambia wengine kwamba wana wa Israeli walipita kwenye maji madogo tu ya futi mbili! Mtoto mdogo akajibu "Haleluya, basi huu ni mwujiza zaidi ya nilivyofikiri, kwa kuwa Waisraeli walipita kwenye maji ya kina cha futi mbili, lakini Wamisri wakazama kwenye futi mbili za maji!". Hakika, hata watoto waliotetemeka kuona jeshi la Farao wakajua ukuu wa Mungu. Kweli Farao aliyekuwa anataka kulipiza kisasi kwa ajili ya mtoto wake aliyekufa, na kupata watumwa wake ili aendeleze ukatili wake, alishughulikiwa na

mkono hodari na wenye nguvu. Mkono huo upo hata leo ili kutusaidia katika shida zetu. Hebu tukumbuke kuombea watoto wetu, wakati wa raha na wakati wa shida.

Hakuna ambaye angeusahau usiku ule. Jinsi walivyokuwa wengi na kuvuka kwa usiku mmoja tu; mifugo na kila kitu chao, lazima kulikuwa na njia pana ili wapite. Musa akaendelea kuwaongoza Israeli waendelee mbele ya Bahari ya Shamu wakatokea jangwa la Shuri na kwenda safari ya siku tatu jangwani wakafika Mara, maana yake 'chungu'. Watu walikuwa wameshikwa na kiu lakini maji yalikuwa machungu. Ndipo watu wakamnung'unikia Musa, naye akamlilia BWANA. BWANA akamwonyesha mti ambao alikata kipande na akakiweka kwenye maji na yakawa matamu. BWANA akaweka amri na hukumu huko, akawajaribu hapo na kuwaambia "Waisikilize kwa bidii sauti ya BWANA Mungu wao na kuyafanya yaliyoelekea mbele Zake, na kutega masikio wasikie Maagizo Yake, na kuzishika Amri Zake, Naye hatatia maradhi yoyote aliyowatia Wamisri; "kwa kuwa Mimi ndimi BWANA nikuponyaye". Hakika Mungu aliwabeba katika mbawa Zake, kama vile tai abebavyo watoto wake. Wakafika Elimu, palipokuwa na chemchemi 12 na mitende 70. Wakapiga kambi karibu na maji wakapumzika baada ya matukio mengi. Kisha wakatoka Elimu na kufika Bara la Sini siku ya kumi na tano ya mwezi wa pili baada ya kutoka kwao nchi ya Misri.

Wimbo huu wa sifa pia utaimbwa na waliookolewa Mbinguni (Ufu 15:3). Mtu anaweza kufikiria kwamba kwa miujiza ya ajabu ya kukombolewa katika Bahari ya Shamu, imani ya Waebrania ingeimarishwa maisha yao yote. Lakini hilo halikutokea. Muda mfupi baadaye, watu walimlalamika Bwana tena. Kwa nini hili lilitokea? Kwasababu hawakuwa wamekuza na kuboresha imani yao; tabia zao bado ziliakisi mazingira waliyotoka. "Walikuwa wametoka Misri, lakini Misri haikuwa imetoka mioyoni mwao, Hata na sisi pia lazima tuondoe "Babeli" (Ufu 17:5) kutoka ndani yetu ili kuingia Kanaani ya mbinguni. Na ni jinsi gani tufanye hivyo? Tabia ya Yesu lazima ikuzwe ndani yetu. Ni kwa kumpenda, kumwiga, na kumtegemea Yeye kabisa, ndipo tutakapobadilishwa kuwa mfano Wake. Yeye Ndiye, Kweli, njia ya uzima wa milele (Yoh 14:6; Isa 45:22).

Nyimbo ni njia maalumu ya kukazia wema wa Mungu na matukio. Katika uumbaji wa ulimwengu, "nyota za asubuhi ziliimba pamoja, na wana wote wa Mungu wakapiga kelele kwa furaha." Ayubu 38:7. Katika kuvuka bahari ya Shamu kulikuwa na kuimba. Malaika waliimba wakati wa kuzaliwa kwa Yesu (Luka 2). Hakika hilo litakuwa mojawapo ya maombi yangu nitakapofika mbinguni, kusikia wimbo huo. Na pia juu ya bahari ya kioo wale wote waliookolewa "wataimba wimbo wa Musa… na wimbo wa Mwana-Kondoo," Ufu. 15:3. Tutamshukuru Bwana kwa kuziweka huru roho zetu kutoka katika utumwa wa dhambi, Mungu ametufanyia ukombozi mkuu kuliko ule wa Waebrania katika Bahari ya Shamu. Maadui wote wa haki wataangamizwa na ushindi wa mwisho wa Israeli wa Mungu utapatikana (Israeli wa kiroho). Je, wewe pia utakuwepo ili kujiunga na kwaya hiyo kuu? Kwa neema ya Mungu, mimi nitakuwepo!

*Hadharani na katika ibada binafsi, pote hapa ni wajibu wetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotuma maombi yetu Kwake. Tendo hili linaonyesha utegemezi

wetu kwa MUNGU.

---

Kulikuwa na nini pale Elimu? Ni nani waliongoza kuimba nyimbo? Waisraeli walivukaje bahari ya Shamu? Nini kilimtokea Farao na jeshi lake? Nani aliuliza "mbona unanililia Mimi?"



**SIKU YA 33**
**( Februari 2)**

# Maji Machungu na Mkate wa Mana - Malalamiko yazidi

**- Kutoka 16.**



Kwenye jangwa hili la Sini hakuna kilichokuwa kinasitawi, na watu wakasahau tena makuu ya Mungu japo waliyaona siku chache tu zilizopita, na wingu na moto lililoonesha kuwa BWANA Mwenyewe Ndiye aliyekuwa anawaongoza. Pengine mmoja alianza kulalamika, akaambukiza wengine. Kukosa imani na manunguniko ni jambo baya sana kwani laweza kuingiza wengi kufanya dhambi. Tukumbuke kutoa shukurani na kumtii Mungu anapotuongoza. Unapokosa imani, mara zingine ni vyema kunyamaza na kuomba kimoyomoyo. Ni kweli walikuwa na watoto, na wanyama wao pia, ila walijisahau kwamba Misri walikuwa utumwani, wakaanza kupatukuza Misri kuliko kukaa katika mikono ya BWANA. Wakasema "laiti tungelikufa kwa mkono wa Bwana katika nchi ya Misri hapo tulipoketi karibu na zile sufuria za nyama, na tulipokula vyakula hata kushiba, kwani mmetutoa huko na kututia katika bara hili, ili kutuua kwa njaa kusanyiko hili lote". Basi wakakumbuka vitunguu saumu, matikiti, matango na mengineyo, na kusahau Ukuu wa Mungu.

Kazi ya uongozi ni nzito. Ni utumishi kwa watu na si ubwana mkubwa kama uongozi mwingine wa kidunia. Mungu anataka viongozi Wake wawe watumishi. Hata Yeye alitumikia watu wakati alipokuja duniani. Hatuwezi kugusa mbingu bila kugusa watu. Kwa kuwa watu waliwaona Musa na Haruni, waliwaelekezea maneno ya lawama, manunguniko na hata kugombana nao! Kuridhika na shukurani ni jambo muhimu sana.

Hata leo Mungu ana watumishi Wake, na tuwe makini, kutofanya maisha yao kuwa ya huzuni kama yalivyokuwa ya Musa. Iwe ni kwa kuwasema, kuwanyanyasa au kutotii mamlaka waliyopewa na Mungu. Ni kweli kuna watumishi wengine ni wa mshahara, bali kuna wengi ambao wanamtumikia Mungu wa mbinguni kwa haki na Kweli. Basi tusifanye kazi yao kuwa ngumu, maana Mungu amewaweka kwa manufaa yetu. Basi BWANA akaahidi kuwanyeshea mvua ya mkate toka mbinguni, na akaagiza kila siku waokote kiasi cha kuwatosha kula kwa siku hiyo tu, na siku ya sita waokote maradufu kujitayarisha kwa siku ya mapumziko ya Sabato. Mungu alitaka kuwapima kama watafuata Maagizo. Walipaswa waokote kiasi cha kuwatosha tu na si kwa ulafi, na siku ya mapumziko ya Sabato wasiokote. Basi Musa na Haruni waliwaambia watu Maagizo ya BWANA, na kwamba wayafuate maana Ndiye aliyewatoa katika utumwa mbaya. Hata leo tumetolewa kwenye utumwa wa dhambi. Dhambi ni Misri ya namna yake, na tusikie sauti ya BWANA na kukaa ndani ya Neno Lake, tushike Maagizo Yake na kutunza siku Yake.

Haruni alizungumza na watu, kisha BWANA akasema na Musa akasema, "Nimesikia manung'uniko ya wana wa Israeli; haya sema nao, ukinena, wakati wa jioni mtakula nyama, na wakati wa asubuhi mtashiba mkate, nanyi mtajua ya kuwa Mimi Ndimi BWANA Mungu wenu. Ikawa wakati wa jioni, kware wakakaribia na kukifunika kituo. Kisha asubuhi umande ulipotoka wakaona kitu kidogo kilichoviringana kama sakitu au utando juu ya nchi. Wana wa Israeli wakaambiana mana, yaani "ni nini hiki". Musa akawaambia ndio mkate ambao BWANA amewapa mle, akarudia maagizo ya kuokota mkate huu. Wakaokota na waliipima kwa pishi. Yeye aliyekuwa ameokota kingi hakubakiwa na kitu, na yeye aliyekuwa ameokota kichache hakupungukiwa. Waliokota kila mtu kwa ulaji wake, wakaambiwa wasitunze au kubakisha. Wengine hawakusikiliza wakakibakisha na asubuhi kilikuwa kina mabuu, na uvundo. Wengine walienda kuokota siku ya Sabato lakini hawakukuta kitu. Musa akakasirika kwani aliwaona wana shingo ngumu za ukaidi, kwa kutosikiliza Amri za BWANA.

Waliendelea kuokota mana, kwa miaka 40 mpaka walipofika kulima na kuvuna ndipo mana iliacha kuanguka. Nguo zao na viatu havikuchakaa. Ahimidiwe BWANA Ambaye Ndiye mtoaji wa vyote, na mwenye upendo mkuu kwetu. Mkate huu waliutengeneza kwa aina mbali mbali. Waliweza kula ulivyo, kuoka na mitindo mingine ya mapishi ukawa una ladha na harufu tofauti tofauti. Hawakuhitaji kufanya kazi ili kupata chakula, walilishwa miaka 40 bure, hata hawakuwa na haja ya kulipa kodi ya nyumba au kununua nguo mpya. Waisraeli walipoanza manunguniko ndipo walipoona chakula hiki hakiwafai, vinginevyo kilikuwa bora na walikipenda. Watoto wengine wakipewa vitu vya kuchezea, wanavikinai haraka, na hutaka vingine. Watoto wengine wadogo wakienda dukani wanalilia vitu na hawataki kutoka mpaka wapate kile wanachokitaka na baada ya siku chache tu

huichoka na kuanza kulilia kingine. Ni vyema kuzungumza na Baba wa mbinguni na kumwambia kwamba "Baba hiki chakula leo kimenikinai, naomba unibadilishie kingine leo", Yeye ni Baba anaelewa,

Mtoto mmoja wa miaka 12 alialikwa kwenye karamu yenye vyakula tofauti zaidi ya mia mbili, kwenye meza mbalimbali, naye akapita huku akilalamika, "mbona hamna kitu ninachokipenda hapa?" Chakula kina sehemu kubwa katika kuwa na tabia njema, kwani tusipotawala tamaa ya chakula ni rahisi kuingia majaribuni. Ndivyo bustani ya Edeni ilivyopotea kwa kutotawala tamaa ya chakula. Kukana tamaa za mwili na macho ni ushindi mkubwa. Leo, tutambue baraka tulizojaliwa badala ya kunung'unika kwa yale yasiyotupendeza katika safari yetu ya kwenda Kanaani ya mbinguni. Hebu tuwe na shukrani kwa upendo na utunzaji Wake! Kila siku mana ilifunika ardhi na kunena ujumbe wa rehema upya kila asubuhi na kama sivyo, wote wangeteketea. Mungu daima amekuwa makini kwa mahitaji ya watoto Wake Utunzaji huo unaonyeshwa vyema katika Yesu, ambaye ni mkuu kuliko mana waliyopewa wana wa Israeli jangwani. "Mimi Ndimi mkate wa uzima" (Yohana 6:48). "Hiki ndicho chakula kishukacho kutoka mbinguni, ili kila mtu akila asipotee" (Yohana 6:50). Katika yote tujue kwamba Mungu Ndiye Mmiliki na Mpaji. Hitaji kuu la ulimwengu ni hitaji la watu-watu ambao hawatanunuliwa wala kuuzwa, watu ambao ndani kabisa ya nia zao ni wakweli na waaminifu, watu wasioogopa kuiita dhambi kwa jina lake halali, watu ambao dhamiri zao ni aminifu katika wajibu kama ilivyo ncha ya dira ya kaskazini, watu watakaosimama kwa ajili ya haki japo mbingu zianguke.

Mana ilikuwa kama chembe ya mtama mweupe na utamu wake kama maandazi membamba yaliyoandaliwa kwa asali. Musa akawaamuru waweke pishi moja kama kumbukumbu ya historia kwa vizazi vijavyo wapate kukiona kile chakula kilichowalisha barani, na kumtukuza Mungu kwa upaji Wake. Haruni akatwaa kopo akaweka pishi moja ya mana ili kuwa ushahidi, ilindwe kwenye madhabahu. Hata leo Mungu anatenda miujiza mikubwa kwetu. Wakati fulani nilikutana na watu 60 toka Angola kwenye mkutano wa walei kule Michigan, nao waliniambia kuwa mana imekuwa ikidondoka kwao Angola, wakati wa njaa mwaka huo! Nilishangaa sana ila walipiga picha watu wakiokota, na vyombo vya habari vikiwahoji walipokuwa wanaokota. Mungu bado anatoa wokovu na msaada, Mana ilipaswa isiokotwe siku ya Sabato, ikimaanisha hata wakati ambapo hatuwezi kununua au kuuza wakati sheria ya Jumapili imepitishwa, Mungu atawalisha watoto Wake waaminifu, kwa maana hata jangwani, Yeye aweza kuleta mvua ya chakula! Hata jangwani, tunapaswa kuikumbuka na kuitakasa "Sabato takatifu kwa Bwana".

*Tunatumaini kwamba ndugu zetu hawataonyesha heshima na kicho kidogo wanapomkaribia MUNGU wa pekee wa Kweli na Aliye Hai kuliko wapagani wanavyoitendea na kujidhihirisha kwa miungu yao ya sanamu, la sivyo watu hawa watakuwa waamuzi wetu katika siku ya hukumu ile ya mwisho. Ningezungumza na wote wanaoshika nafasi ya waalimu katika shule zetu. Wanaume na wanawake, msimdharau MUNGU kwa kutomheshimu kwenu kwa kujigamba, huku mkijionyesha ufahari na umuhimu wenu. Usisimame katika Ufarisayo wako na kutoa maombi yako kwa MUNGU. Usiamini nguvu zako mwenyewe. Usizitegemee; lakini mara

kwa mara pigeni magoti mbele za MUNGU, na mmwabudu Yeye

---

Nini kilitokea walipokunywa maji machungu? Waisraeli walikumbuka vyakula gani vya Misri? Je, ulafi una ubaya gani? Nini maana ya Mana? Kwa nini waliambiwa wasiokote mana siku ya Sabato? Walikula Mana miaka mingapi? Je, Mungu anatupatiaje chakula siku hizi? Waweza kuorodhesha mema Mungu aliyokutendea?

**SIKU YA 34**
**( Februari 3)**

# Maji ya Meriba na Kugawanya Uongozi

**- Kutoka 17 na 18**

Basi wana wa Israeli wakasafiri kwenye Jangwa la Sini na kufika Refidimu, na hapo hapakuwa na maji. Wakamjaribu Musa kwa kumwambia "tupe maji tunywe." Musa akasema kwa nini wanagombana naye? Watu wenye kiu wakasema "umetuleta kutuua sisi na watoto wetu na wanyama wetu". Musa akamlilia BWANA akisema, "niwatendee nini watu hawa bado kidogo watanipiga kwa mawe. BWANA akamwambia Musa achukue baadhi ya wazee wa Israeli na ile fimbo aliyopiga nayo mto Nile, kisha aende kwenye jabali la Horebu, na huko BWANA atakuwapo na apige jabali mara moja na maji yatatoka wapate kunywa. Musa alifanya vile na akapaita pale Masa na Meriba kwa ajili ya mateto ya wana Israeli, kwa sababu walimjaribu wakisema "Je, BWANA Yu kati yetu au siyo?"



Wakati huo Waamaleki wakatokea na kupigana na Waisraeli. Musa akamwambia Yoshua achague watu ili waende wakapigane nao, naye akasimama kwenye kilele na fimbo ile ya Mungu. Basi walipigana na Waamaleki, na Musa, Haruni na Huri wakapanda kilima. Ikawa Musa alipoinua mikono yake Israeli walishinda na aliposhusha, Israeli walishindwa. Mikono yake ilikuwa imechoka na hivyo wakatwaa jiwe akalikalia na Huri na Haruni wakaitegemeza mikono yake ikathibitika hata jua lilipokuchwa. Yoshua akawaangamiza Amaleki na watu wake kwa ukali wa upanga wa nguvu za BWANA. BWANA akamwambia Musa aandike haya kwenye kumbukumbu, iwe ukumbusho. Kisha akamwambia Yoshua "nitaufuta ukumbusho wa Amaleki kabisa, usiwe tena chini ya mbingu". Musa akajenga madhabahu, akaiita Yehova-Nisi, yaani "BWANA Ameapa; BWANA atakuwa na vita na Amaleki kizazi baada ya kizazi". Inaonekana dhambi za watu hawa zilikuwa zimefurika kikombe, na ilibidi Mungu atoe adhabu kwao. Hata leo inabidi tushike mikono ya watendakazi wa Mungu ili kuwategemeza, tusiwe wachoyo wa muda, hali na mali.

Yethro kuhani wa Midiani na mkwe wa Musa alisikia habari ya matendo makuu ya BWANA kwa Musa na wana wa Israeli, naye akaja kumwona Musa akiwa pamoja na mke wa Musa, Sipora, baada ya yeye kumrudisha wakati alipoenda kumwona Farao. Yethro akamwendea Musa na wajukuu zake au watoto wawili wa Musa, Gershomu (mimi ni mgeni) na Eliezeri (Mungu ni msaada wangu). Musa alikuwa

Horebu, au mlima wa Mungu (Sinai) pale alipoona kijiti kinawaka moto, na Musa akatoka ili kumlaki mkwewe, akasujudu na kumbusu, na wakaulizana habari, kisha wakaingia hemani. Musa akamwelezea Yethro matendo makuu ya BWANA aliyomtenda Farao na Wamisri, na mambo mazito yaliyowapata njiani na jinsi BWANA alivyowaokoa. Yethro akafurahi kwa ajili ya wema wa BWANA na akasema, "Ahimidiwe BWANA aliyewaokoa mikononi mwa Wamisri na mkono wa Farao…. sasa najua BWANA ni mkuu kuliko miungu yote". Tunapofanyiwa mema na BWANA tusikose kuwaeleza wengine. Hii inawasaidia hata wao kufurahi na kujua kuwa BWANA ni mweza mwenye upendo na Aliye tayari kutusaidia katika dhiki zetu. Ushindi wetu dhidi ya Shetani ni kwa kwa damu ya Mwana- Kondoo. Basi Yethro akamletea Mungu sadaka ya kuteketezwa na dhabihu, kumshukuru Mungu kwa matendo Yake makuu na ya ajabu.

Kisha Haruni na wazee wa Israeli wakaja wale chakula pamoja na mkwe wa Musa mbele za Mungu. Asubuhi yake Musa aliketi kama hakimu ili awasaidie watu na kesi zao. Watu walisimama kumzunguka Musa, asubuhi mpaka jioni. Mkwewe Musa alipoyaona haya alimwuliza, ni nini kinachoendelea? Musa akasema, "Ni kwa sababu watu hunijilia mimi wapate kumwuliza Mungu, wakiwa na neno … naamua kati ya mtu na mwenziwe na nawajulisha Amri za Mungu na Sheria Zake". Yethro akamshauri akasema, "Jambo hili ufanyalo si jema. Huna budi utadhoofika wewe na hawa watu walio pamoja nawe pia, maana jambo hili ni zito mno kwako, huwezi wewe kulitenda peke yako". Akampa ushauri wa kuwasaidia watu wake na kuwajulisha Sheria na Amri za Mungu na kuwaonyesha njia waipasayo kuiendea, na kazi za kufanya, ila ajipatie watu wenye uwezo, wenye kumcha Mungu, watu wa Kweli. Watu wenye kuchukia mapato ya udhalimu; aweke mikono juu yao, ili wawe wakuu wa maelfu, mamia, hamsini na kumi. Hawa waamue siku zote, kisha wakuletee wewe neno kubwa tu, ila madogo wataamua wenyewe. Akakazia kwamba hii itampa muda wa kutosha na wao watamsaidia kubeba mzigo. Akamwambia Mungu akikubali achukue ushauri huu, na itasaidia watu washughulikiwe kwa haraka. Musa alipokea ule ushauri kwa moyo mkunjufu, akafanya yote aliyoambiwa. Alichagua viongozi wa maelfu, mamia, hamsini na kumi, wenye uwezo nao wakaamua watu siku zote, na kuleta tu yale mashauri yaliyokuwa magumu. Musa akaagana na mkwewe, na Yethro akarudi Midiani.

Kisa hiki kinatuonesha unyenyekevu wa Musa na pia hekima ya kuona kwamba kama binadamu huwezi kila kitu, unahitaji msaada wa wengine, la sivyo utaanguka kwa uzito wa mambo. Musa alijaribu kumvuta shemejiye Hobabu au kaka wa Sipora aende nao nchi ya ahadi. Alimwambia "usituache tafadhali, kwa kuwa wewe wajua jinsi tutakavyopanga nyikani, nawe utakuwa kwetu badala ya macho…itakuwa mema yoyote Bwana atakayotutendea sisi, tutakutendea wewe vivyo". Hii ni ajabu kwa kuwa Musa aliongozwa na Mwenye uwezo wote, na elimu yote, kwa wingu na moto. Pengine alitaka tu kufuatana na shemeji yake mpendwa!

*Kote hadharani na katika ibada binafsi ni wajibu wetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapoyaleta maombi yetu Kwake. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Juu ya wanafunzi Wake." Imeandikwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu

Kristo magoti." Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, na kushukuru mbele za MUNGU wake."

---

Nini kilitokea penye maji ya Meriba? Kwanini ilikuwa dhambi kubwa? Musa aliponyanyua mikono yake jambo gani lilitokea? Nani aliinua mikono ya Musa? Baba mkwe wa Musa Yethro alitoa ushauri gani kwa Musa? Unafikiri ni kwa nini Musa aliomba Hobabu awasindikize wakati nguzo ya moto usiku na wingu mchana ilikuwa ikiwasindikiza?

**SIKU YA 35**
**( Februari 4)**

# Amri Kumi Katika Mlima wa Sinai (Horebu)

**- Kutoka 19 na 20**



Mlima Sinai, ambao pia unaitwa mlima wa Mungu upo Misri. Mwezi wa tatu baada ya kutoka Misri Waisraeli walifika jangwa la Sinai, wakapiga kambi wakiukabili mlima. BWANA akamwita Musa kutoka kwenye ule mlima na kusema, "Utawaambia wana wa Yakobo na kuwaarifu Waisraeli…mmeona jinsi nilivyowatendea wamisri na jinsi Nilivyowachukua ninyi juu ya mbawa za tai" Akawaagiza waitii sauti Yake kweli kweli, na kulishika Agano Lake, hapo ndipo watakapokuwa tunu Kwake kuliko makabila yote ya watu, maana dunia yote pia ni mali Yake. Akawaambia watakuwa ufalme wa makuhani na taifa takatifu.

Musa akawaita wazee wa Israeli na kuwafunulia Maneno ya BWANA yote aliyoagiza. Watu wakaitika pamoja wakisema, "hayo yote Aliyosema Bwana tutayatenda". Naye Musa akamwambia BWANA kiitikio cha watu hao. BWANA akasema atasogea ili watu wamsikie atakaposema na Musa, ili watu wamwamini Musa pia. BWANA akamwambia Musa awaambie watu waende wakajitakase siku hiyo na kesho yake na wazifue nguo zao, na kuwa tayari, na siku ya tatu atashuka katika mlima Sinai machoni pa watu wale wote. Akamwambia aweke mpaka pande zote chini ya mlima, na watu wajihadhari wasipande mlima, wala wasiguse mapambizo yake. Akasisitiza, kila mtu au mnyama atakayeugusa mlima huu atauawa, kwa mawe au mkuki. Wakapewa maagizo pale panda itakapotoa sauti ya kufuliza ndipo wakaribie mlima. Musa akashuka mlimani, akawaambia watu wajitakase na kufua nguo, na kutokuwa na mahusiano ya ndoa kwa siku tatu.

Siku ya tatu asubuhi palikuwa na ngurumo na umeme na wingu zito juu ya mlima na sauti ya baragumu iliyolia sana. Watu waliokuwa chini ya mlima woga ukawaingia wakatetemeka, Musa akawatoa kwenye kituo waonane na Mungu. Wakasimama chini ya mlima, na mlima ukatoa moshi kwa sababu Bwana alishuka katika moto na moshi ukapada juu kama kwenye tanuru, na mlima wote ukatetemeka sana. "BWANA akashuka kwenye kilele cha mlima" na kumwita "Musa". Musa akapanda kileleni na ndipo BWANA akamwambia ashuke na awaonye watu Wake wasije wakalazimisha kuja juu kutazama na kuangamia. Makuhani nao walipaswa

kujitakasa ili wamkaribiapo BWANA wasije wakapatwa na ghadhabu. Bwana akamwambia Musa na Haruni wapande juu bali makuhani na watu wasije juu.

Mungu akanena Amri kumi akiwakumbushia kwanza mema makuu na upendo Wake: Akasema "Mimi ni Bwana Mungu niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa". (Hii ni ahadi na wema wa Mungu, na ni vyema kuelewa kwa sababu wengi wanazungumza Amri kumi bila kutilia maanani kwamba BWANA amekutukumbusha kwamba ametutoa katika nyumba ya utumwa wa dhambi, kabla amri hazijatamkwa, Mungu alikuwa ametuonesha upendo wake mwingi. Shetani ni mnyapara mwenye ukatili na uonevu mwingi. Mungu atusaidie tuepuke utumwa wake.



1. **"Usiwe na miungu mingine ila Mimi." Hii inaonesha kuwa Mungu awe wa kwanza katika maisha yetu. Tunavyotumia muda wetu, mali zetu, karama, miili au chochote, Yeye awe wa kwanza.**
2. **"Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia, kwa kuwa mimi Bwana Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu, nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao na kuzishika Amri Zangu." Siku hizi kuna miungu mingi ambayo haichongwi. Miungu hii ni kama vile michezo au vitu vya kuchezea, kazi, tumbo, mke, mtoto, kompyuta, gari, nyumba, uzuri, maoni, fikra, vitu, mali, fasheni, urembo, uzuri, elimu, burudani, mvuto, n.k. Kwa jumla maswali ya kujiuliza ni haya mane,**
   **Je, Ninatumia Wakati Wangu Wapi?**
   **Je Pesa Zangu Ninatumia Wapi?**
   **Je, Ninajipatia Furaha Yangu Wapi?**

**Ni Nini Kipo kwenye mawazo au moyo wangu Kila Wakati?**

3. **"Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako, maana Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina Lake bure. Hatupaswi kuapa "haki ya Mungu", Kweli yetu iwe Kweli, inatosha. Kutaja jina la Mungu bure pia ni kusema kuwa tu wana Wake ila matendo yetu ni maovu, hayamwakilishi vyema, hivyo watu wanadharau jina Lake kwa sababu ya matendo yetu.**
4. **"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase, siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote. Lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yoyote wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa kwao, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi na bahari na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa." Amri hii ndiyo ndefu kwa maandishi, na inaonekana kuwa utumwani wana wa Israeli walisahau kutunza siku ya Sabato hivyo walikumbushwa tena. Isaya 58 anasema siku hii si ya kufanya anasa na shughuli zetu. Tuifanye ya kupendeza na si ya utumwa, tukichukia kwenda ibada au kwamba kuchwe haraka ili tuendelee na kazi zetu. Ni siku ya mahusiano Naye. Siku hii ni ya ibada kumwabudu aliyetuumba na kutenda matendo mema.**

   **'siku ya kwanza ya juma' ni siku ambayo Yesu alifufuka kutoka kwa wafu." Inaendelea kuorodhesha Marko 16:2, Luka 24:1, Yohana 20:1, Mathayo 28:1, Marko 16:9–20 na Yohana 20:19 kama uthibitisho wa madai hayo ambayo inatueleza bila kipingamizi kwamba Sabato ni Siku gani.**
5. **"Waheshimu baba yako na mama yako ili siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako." Amri hii ndiyo pekee yenye ahadi. Ni muhimu sana kuheshimu wazazi na wakubwa wetu. Kuna wale ambao wamepata shida kwa kuwa na wazazi 'wenye tabia ngumu,' lakini bado Mungu anasema tuwaheshimu. Hata hivyo maagizo yao yakitofautiana na Mungu, Matendo 5:29 inatuagiza kwamba, "imetupasa kumtii Mungu kuliko mwanadamu". Wakiwa wazee usiache wazazi wako wataabike wakati una uwezo wa kuwatunza, wapende na usione aibu kuwatambulisha kwa marafiki zako.**
6. **"Usiue": Hii ndiyo Amri fupi kupita zote, ila ina uzito wake katika Amri sita za mahusiano kati yetu sisi kwa sisi. Amri hii ipo kwenye mahakama zote duniani. Kristo aliongeza kwamba hata kuwa na chuki na mtu ni kuua pia, pengine hatujapata nafasi kumwua mtu au tunaogopa adhabu. Tuungame, tusiache chuki itumalize, kisha tumwambie Mungu atusaidie itutoke.**
7. **"Usizini": Amri hii inasimamia kutofanya uasherati au uchafu wa ngono wa aina yoyote. Mtu asiwe asifanye ngono na yoyote isipokuwa ndani ya ndoa. Jitunze kwa mawazo, maneno na matendo. Epuka mambo yatakayokufanya uingie katika dhambi hii, aidha kwa kuzungumza na jinsia nyingine mafichoni au gizani pasipo na watu. Kumtamani mke au mume asiye wako ni kuzini pia.**
8. **"Usiibe": Kuchukua chochote kisicho chetu, au kuazima bila**

**kurudisha ni wizi.**
**Tunaweza kuwa wezi wa muda kwa kutofanya kazi tunapotakiwa au wezi wa kalamu.**
**Kuna wizi wa aina nyingi, hebu tujipeleleze.**

9. **"Usimshuhudie jirani yako uongo". Mtu mmoja alisema, "mimi sina dhambi", mwingine alijibu hapo hapo umefanya dhambi kwa kusema uongo kwa kuwa "kila mtu amefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Hivyo tuungame kwa toba ya kweli na kuomba nguvu za kuishi maisha ya utakatifu. Tunasema uongo kwa njia nyingi, hata kwa kunyamaza bila kusema ukweli tumesema uongo. Kwa ishara za kukonyeza, kutumia mkono, kutia chumvi, kashfa, kupotosha ukweli,kuharibu sifa ya mtu kwa maneno ambayo huna uhakika nayo.**
10. **"Usitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako, wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako." Inawezekana mara nyingi tuna wivu bila kujua kuwa tunao. Moyo ni mdanganyifu. Hebu ufurahi mwenzako akifanikiwa na wala usimtakie au kumtendea mabaya.**

Amri nne za kwanza zilihusika na uhusiano wetu na Mungu na zile sita zinazofuatia ni uhusiano wetu na binadamu wenzetu. Yaani tumpende Mungu kwa mioyo yetu yote, akili zetu zote, nguvu zetu zote na roho zetu zote na nyingine 'inayofanana na hiyo' Biblia inasema ni tumpende jirani kama nafsi. Zinahusiana! Hatuwezi kumgusa Mungu bila kugusa watu. Amri hizi mbili ndiyo muhtasari ya maandiko ya Mungu. Sheria za Mungu si mashauri kumi au maoni kumi bali ni amri 10, Maagizo Yake, Sheria Yake. Dhambi ni kuasi Sheria hizi. Sheria ni kioo cha kujiangalia ni wapi pa kusahihisha. Ziliandikwa kwa mawe zidumu milele. Wengine wanasema ni za Agano la Kale! Hapana. Mbingu na dunia zitatoweka lakini si hizi, ni za milele. Tusichanganye na sheria za kafara zilizohusika na kafara tunazosoma katika kitabu cha Kutoka na Mambo ya Walawi. Hizi zilikoma baada ya Yesu kufa msalabani.

*Kupiga Magoti Katika Maombi Hufunza Heshima na Kumcha MUNGU na kustaajabia Utukufu Wake— Hebu MUNGU na awafundishe watu Wake jinsi ya kuomba. Hebu walimu katika shule zetu na wahudumu katika makanisa yetu, wajifunze kila siku katika shule ya Kristo. Ndipo wataomba kwa bidii, na maombi yao yatasikilizwa na kujibiwa. Ndipo Neno litatangazwa kwa nguvu.


---

Amri nne za kwanza zinasemaje? Amri sita za mwisho zinasemaje? Amri mbili kuu zinasemaje? Dhambi ni nini? Kwa nini amri kumi ni zaidi ya ushauri bora tu? Kwa nini amri ni za milele na si za wakati fulani tu? Kwa nini Sheria inaitwa ni kioo? Kuna tofauti gani kati ya Sheria za kafara na Amri kumi?

**SIKU YA 36**
**( Februari 5)**

# Sheria na Hukumu

**- Kutoka 20 na 21**




Mungu alipomaliza kunena Amri Kumi, watu waliona umeme na ngurumo na sauti ya baragumu na ule mlima ukitoka moshi, watu wakatetemeka na kusimama mbali. Wakamwambia Musa, "Sema nasi wewe nasi tutasikia, bali Mungu asiseme nasi tusije tukafa. Musa akawaambia watu wasiogope "maana Mungu amekuja ili awajaribu na utisho Wake uwe mbele yenu, ili kwamba msifanye dhambi." Watu wakasimama mbali, Musa akakaribia lile giza Mungu alipokuwa na Bwana akamwambia Musa awaambie wana wa Israeli kwamba wameona akinena nao mwenyewe toka mbinguni kwa hiyo wasifanye miungu ya fedha, wala dhahabu. Akamwambia Musa afanye madhabahu ya udongo na kutoa dhabihu zake juu yake, sadaka ya kuteketezwa, na sadaka ya amani (kondoo na mbuzi) kila mahali atakapotia ukumbusho wa Jina Lake. Akaambiwa kujenga madhabahu ya mawe yasiyochongwa. Kisha apandapo madhabahuni asipande kwa ngazi ili uchi wake usidhihirike juu Yake.

Mungu akatoa maelekezo ya mahusiano ya kuishi. Sheria hizi tunaweza kusema ni kama taa za kuongoza magari barabarani ili yasipate ajali au shida. Tutaangalia mifano michache: Mtu aliyenunua mtumwa wa Kiebrania, atamtumikia miaka

sita ila mwaka wa saba aachiwe huru kwenda, ila kama alipata watoto na familia akiwa huko basi wale wana watakuwa wa yule bwana, ila yule mtumwa akisema anampenda mke na watoto wake basi atakuwa bado chini ya huyu bwana. Basi amlete huyu mtumwa malangoni na kuapishana naye kwa kutoboa sikio lake ili amtumikie siku zote. Mungu akaendelea kutoa Sheria za kuishi pamoja kama vile mjakazi atakavyofanyiwa pale alipo kwa haki. Akazungumzia mtu kumwua mtu kwa kumvizia, basi auawe, au yeye ampigaye baba au mama yake auawe. Naye amwibaye mtu na kumwuza akipatikana atauawa. Na endapo mtu atampiga mtu mpaka akawa hoi kitandani na akainuka akitembelea fimbo atalipa fidia. Akamwambia Musa jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu, kuteketeza kwa kuteketeza, jeraha kwa jeraha na chubuko kwa chubuko. Hata ng'ombe wa mtu akimpiga mtu pembe na mtu huyo akafa, ngombe huyo atauawa kwa kupigwa mawe na nyama yake isiliwe, ila mwenye ng'ombe ataachiliwa. Ila kama ng'ombe alizoea kupiga watu na mwenye ngombe asimzuie na mwishowe akaua watu, basi naye atauawa. Maelekezo ya kuposa msichana yaliyotelewa pia, na ya kumtendea na jinsi ya waume kuhusiana na wanawake. Naye achimbaye shimo asilifunike, na mnyama akatumbukia, atalipa huyo mnyama. Naye aibaye mnyama wa mtu atalipa fidia mara tano. Naye mwizi akikutwa anaiba akapigwa na kufa, hatia itakuwa juu yake mwenyewe. Nao wenye mifugo waangalie mifugo yao isilishe kwenye mashamba ya watu. Mtu akiwasha moto na ukaharibu vitu vya mtu, atalipia. Na mtu akimpa mtu amtunziye kitu, na kikaibiwa, atalipa na kama si yeye amechukua, watamwuliza BWANA na hatua itachukuliwa. Na mtu akiazima mnyama wa mtu na akafa, basi atalipa. Mtu asikae na mwanamke bila kuzungumza na wahusika na kutoa mahari. Mchawi atauawa, kwani hapaswi kuishi. Binadamu yeyote asilale na mnyama. Yeyote atakayetoa dhabihu kwa miungu mingine anapaswa kuangamizwa. Mgeni asionewe, kwani na wao walikuwa wageni katika nchi ya Misri. Umkopeshapo mtu maskini, usikae ukimdai dai saa zote, au kumtoza faida.

Usimtukane Mungu na wala usimlaani mkuu wa watu wako. Mwanamume asivae nguo zinazofanya aonekane kama mwanamke na mwanamke asivae ili aonekane kama mwanamume, kwani ni machukizo kwa Mungu, kwa vile wapagani walifanya vile kwa madhumuni mabaya na pia walitaka kuondoa tofauti za mume na mke. Mazao yako ya kwanza na mzaliwa wako wa kwanza wa kiume ni vya BWANA. Usivumishe habari za uongo, na kuwa dhalimu au kupotosha hukumu kwa kula rushwa. Utalima miaka sita na wa saba, utaacha nchi ipumzike na kutulia, na maskini watakula toka humo. "Tazama Mimi naweka Malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale alipokutengenezea … jitunzeni mbele Yake na mwisikize sauti Yake". Wakapewa wosia ili BWANA awashugulikie adui zao, na kuwafikisha Kanaani. BWANA atawarithisha nchi pole pole, kwa vile kuna wanyama wakali na hivyo wasiwe wachache na kukabiliwa na wanyama hawa. Wakakumbushwa wasisujudie miungu mingine na kuitumikia. Naye BWANA atabariki chakula, na maji yao na kuondoa magonjwa kati yao. Kisha wakaambiwa nchi na mipaka watakayopewa na kuonywa wasifanye maagano na wenyeji pamoja na miungu yao, na wala wasikae katika nchi yao wasije wakawafanya kumtendea Mungu dhambi.

*Kote hadharani na katika ibada binafsi ni wajibu wetu kupiga magoti mbele za MUNGU tunapoyaleta maombi yetu Kwake. Yesu, mfano wetu, “alipiga magoti na kuomba.” Juu ya wanafunzi Wake.” Imeandikwa kwamba wao pia, “walipiga magoti na kuomba.” Paulo alitangaza, “Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti.” Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Danieli “alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, na kushukuru mbele za MUNGU wake

---

Kwa nini watu walitetemeka waliposikia ngurumo? Jadili mifano sita ya Sheria za mahusiano za Waisraeli? Kwa nini Bwana angewarithisha Israeli nchi pole pole? Sheria gani leo za nchi zinafanana na Sheria za Waisraeli?


**SIKU ya 37**
**( Februari 6)**

# "Wanijengee Patakatifu"

**- Kutoka 24-27**



BWANA akamwambia Musa na Haruni, pamoja na vijana wake wawili wa kwanza, Nadabu na Abihu, watu sabini wa wazee wa Israeli wakaribie kwa BWANA na kusujudia kwa mbali, na kisha Musa akaribie. Musa akaenda na kuwaambia watu hukumu za BWANA nao wakasema, "yote aliyoyanena BWANA, tutayatenda". Naye Musa akaandika maneno yote ya BWANA, na akaondoka asubuhi na mapema na kujenga madhabahu chini ya mlima, na kumchinjia BWANA sadaka za amani. Musa akatwaa nusu ya damu na kuinyunyiza kwenye madhabahu, kisha akatwaa kitabu cha Agano na kukisoma masikioni mwa watu akisema, "hii ndiyo damu ya Agano alilolifanya BWANA pamoja nanyi katika Maneno yote. Basi Musa, Haruni, Nadabu na Abihu na watu sabini wakakwea juu ili kuonana na Mungu wa Israeli. "Chini ya miguu Yake palikuwa na kama sakafu iliyofanyizwa kwa yakuti samawi, kama zile mbingu zenyewe kwa usafi wake…Naye hakuweka mkono Wake juu ya hao wakuu wa wana wa Israeli, nao wakamwona Mungu, wakala na kunywa". Soma zaidi kuhusu mambo yalivyokuwa siku hii kwenye Biblia. BWANA akamwambia Musa aende mlimani, na akampa mbao mbili za mawe za Amri Kumi,



ili awafundishe. Aliandika kwa chanda cha mkono Wake Mwenyewe. Ndiyo sehemu pekee ambayo Mungu aliandika kwa chanda Chake Mwenyewe, isipokuwa pale Kristo alipoandika mchangani, watu walipomshtaki Mariamu Magdalena.

Musa aliondoka na Yoshua mtumishi wake, na akapanda mlima wa Mungu Horebu (Sinai) na akawaambia wazee wamngoje mpaka atakaporudi, na akawaachia uongozi Haruni na Huri watu waje kwao wakiwa na shida. Wingu likamfunika Musa na utukufu wa BWANA ukawa juu ya mlima kwa siku sita, na siku ya saba Mungu akamwita Musa atoke kwenye lile wingu. Musa akaingia ndani ya wingu hilo kwa siku 40 mchana na usiku. Kisha BWANA akanena na Musa kwamba awaambie wana wa Israeli watoe sadaka "kila mtu ambaye moyo wake wampa kupenda". Sadaka hii ilikuwa ni dhahabu, fedha, shaba, nyuzi za rangi ya samawi, zambarau, na nyekundu, sufi ya kitani safi, singa za mbunzi na ngozi ya kondoo wanaume zilizotiwa rangi nyekundu, ngozi ya pomboo, miti ya mshita na mafuta ya ile taa na viungo vya manukato kwa yale mafuta ya kupaka, na kwa ule uvumba wenye harufu nzuri. Vito vya shohamu, na vito vingine vya kutiwa kwa naivera, na kwa kifuko cha kifuani.

BWANA akatoa maagizo akisema, "Na wanifayie Patakatifu, ili nipate kukaa kati yao." Akawapa maagizo jinsi ya kujenga Patakatifu. Kusudi kubwa la nyumba ya ibada, au kanisa ni kuweza kukaa pamoja na Mungu na kisha kuwa kielelezo cha njia ya kuondoa dhambi kwa kuungama na kutoa sadaka. Jengo hili lilikuwa mfano au kivuli cha mahali Patakatifu pa mbinguni. Hekalu hili la duniani, lilikuwa ni mfano wa lile la mbinguni na huduma zilizokuwa zinaendelea pale zingefanana na

zile zinazoendelea kule juu mbinguni. Akatoa vipimo vya mti wa mshita. Haikuwa nyumba ya umaridadi sana ila ilikuwa mfano wa kule mbinguni. Musa alikaa muda akiambiwa kwa makini vipengele vyote vya kuijenga. Mungu hakuhitaji sana mahali pa kukaa ila kama binadamu tunahitaji mahali pa kujifunza upendo wa Mungu, sheria Yake na wokovu unavyofika kwetu. Hekalu ni picha ya mpango wa wokovu. Alitaka kuwafundisha jinsi anavyochukia dhambi na jinsi ya kuondokana na dhambi ili tuwe safi na wenye haki. Ua wa nje ulikuwa na sehemu ya kutoa kafara, madhabahu, na sehemu ya kunawa kuhani kabla ya kutoa kafara.

Hema ya kukutania, au hekalu lilibebwa kila waliposafiri. Paa na mapazia yake yalikuwa ya rangi za bluu, zambarau, dhahabu na nyekundu. Kila rangi iliwakilisha kitu fulani. Kwa mfano bluu iliwakilisha sheria ya Mungu, nyekundu damu iliyomwagika ya kafara, na zambarau, ufalme. Vipimo vyake vilikuwa urefu wa futi 50 kwa upana wa futi 18 na kenda juu futi 18. Ilikuwa na mbao 48. Patakatifu palitenganishwa sehemu mbili kwa rangi ya bluu, zambarau na nyekundu. Sehemu moja iliitwa Patakatifu na ya pili Patakatifu pa Patakatifu. Sehemu ile ya Patakatifu ilikuwa na mikate ya wonyesho, madhabahu ya chetezo cha kufukizia uvumba na kinara cha taa. Mkate ukionyesha kwamba Mungu Ndiye anatupatia riziki au mkate wetu wa kila siku, na moshi ule ukiwakilisha harufu ya manukato ya upendo wa Mungu ukichanganyika na maombi ya watakatifu yakienda kwenye kiti cha enzi. Vinara saba vya taa ambayo iliwaka wakati wote ilionesha kuwa Mungu ni mwanga na Kweli inayong'aa milele. Ndani katika mahali patakatifu pa Pakatifu palikuwa na sanduku la mti wa mshita lililopakwa dhahabu na ndani yake kulikuwa na mbao mbili za ushuhuda (Amri Kumi). Sanduku hili liliitwa sanduku la Agano kwa ajili ya Amri. Kiti cha rehema kiliwekwa juu ya Sanduku la Agano, na makerubi wawili wakitazama kwa kicho Sheria ya Mungu. Makerubi waliinua mabawa yao juu, na kukifunika kiti cha rehema kwa mabawa yao na nyuso zao zikielekeana. Hapa Mungu angeliwatokea kwa utukufu na kuzungumza nao. Mungu aliweka kiti cha rehema kati Yake na Sheria, akitaka watu waone kwamba yupo tayari kuwasamehe, kama wakiomba msamaha na kuwa na toba ya kweli. Fimbo ya Haruni na Mana pia ilikuwa kwenye sehemu hii ya Patakatifu pa Patakatifu. Mbele ya Patakatifu kulikuwa na birika la shaba lenye maji la makuhani kujisafisha kabla ya kuhudumu na madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa.

Hema hii ilitolewa kama mfano wa hema ya mbinguni. Mbinguni tunaambiwa kwa uwazi kuwa kuna hema. Kitabu cha Waebrania chote kinaelezea vizuri hema ya mbinguni, na Kristo Ndiye Kuhani, na mtetezi wetu kwenye ile hema. Tunaambiwa tuwe na ujasiri kumwendea Yeye, tukiungama dhambi zetu maana anaweza kutuokoa katika uovu wetu, maana anahudumu katika hema hiyo.

Kisha Mungu akamwambia Musa huduma zitakazofanyika hekaluni, na jinsi wanyama watakavyotolewa kafara. Si kwa sababu Mungu anafurahia kafara zikitolewa Kwake, bali ili binadamu tuone jinsi dhambi ilivyokuwa ya kuchukiza kwake, na kuwa mshahara wake ni mauti. Hivyo mwenye dhambi alipaswa kumchinja mwana-kondoo asiye na hatia, ili kuonesha kwamba alipaswa kufa yeyé lakini mwana-kondoo amekufa badala yake. Mwana-kondoo huyu alimwakilisha Kristo ambaye siku moja angekufa Kalvari kama "Mwana-Kondoo wa Mungu,

aichukuaye dhambi ya ulimwengu". Hivyo Musa akakaa siku 40 kule mlimani. Mungu akamwambia kile alichotaka akifanye, hata akampa majina ya wale ambao wangekuwa makuhani na kuelekeza jinsi nguo watakazovaa na nakishi zake zitakavyokuwa. Bwana akarudia tena Amri hizo mara ya pili. Kisha baada ya siku 40 za kuzungumza na Bwana Mungu, Bwana akamkabidhi Musa mbao mbili za mawe zilizoandikwa Amri Kumi.

*Kumcha MUNGU katika kweli kunachochewa na hisia ya ukuu Wake usio na kipimo na utambuzi wa uwepo Wake. Kwa hisia hii ya Yule Asiyeonekana, kila moyo unapaswa kuvutiwa sana. Saa na mahali pa maombi ni vitakatifu, kwa sababu MUNGU Yupo; na kadri heshima na kicho inavyodhihirika katika tabia na mwenendo, hisia inayovichochea itazidishwa." Jina Lake ni takatifu na la kuogopwa," mwandishi wa Zaburi anatangaza. Malaika, wanaponena Jina hilo, hufunika nyuso zao. Kwa heshima gani, basi, sisi ambao tumeanguka na ni wenye dhambi, tunapaswa kulichukua kwenye midomo yetu!

---

Hema ya kukutania ilikuwa kwa ajili gani? Taja sehemu tatu za hema? Taja fanicha sita za madhabahu? Rangi ya zambarau, nyekundu na bluu zilisimamia nini? Je, kumchinja mwana- kondoo kilikuwa kivuli cha nini? Hema ya kukutania ilikuwa picha ya wokovu kwa mwanadamu, jadili hili. Kitabu cha Waebrania 8 na 9 kinasema hema hii ni mfano wa ile ya mbinguni. Je, mbinguni nani ni kuhani? Kwa nini ni muhimu nasi kusamehe watu na kujisamehe wenyewe?

**SIKU YA 38**
**( Februari 7)**

# Dhambi ya Kuabudu Ndama wa Dhahabu

**- Kutoka 32 na 33**

Basi Musa akashuka kutoka mlimani. Mungu alimdokeza kwamba wana wa Israeli wameasi, “shuka, kwa maana watu wako uliowatoa katika nchi ya Misri wamejiharibu nafsi zao, wamepotoka upesi na kuiacha ile njia…wamejifanyizia ndama … wakaiabudu na kuitolea dhabihu.” Hata hazikuwa zimepita siku 40 toka kusikia sauti ya Mungu akiwaambia Amri Kumi, lakini walikuwa wamesahau. Hili ni fundisho kwetu tusisahau Maagizo ya Mungu. Na tuwe wanyenyekevu. Musa akasikia sauti za ajabu kama watu wanaoimba na mara macho yake yakaona sanamu ya ndama wa dhahabu. Yoshua alikuwa amemngoja kwa chini kidogo naye akafikiri watu wanapigana vita. Kumbe watu walipoona amekawia kushuka chini walimwendea Haruni na kusema, “Haya! katufanyizie miungu itakayokwenda mbele yetu, kwa maana Musa huyo aliyetutoa katika nchi ya Misri hatujui yaliyompata”. Inaonekana Mzee Haruni alikuwa na udhaifu wa tabia, na kuogopa watu. Basi akawaambia wavunje pete zao za dhahabu zilizo katika masikio ya wake zao na watoto wao na kumletea. Walipomletea, akatengeneza sanamu ya ndama kwa kuiyeyusha! Na watu wakasema huyu ndiye mungu wao aliyewatoa Misri. Kutengeneza kitu kama hiki kinachukua muda mrefu, na hivyo ni dhambi ya kudhamiria. Haruni akajenga madhabahu na kutangaza kuwa siku inayofuata itakuwa sikukuu kwa BWANA. Mara nyingi walitaka kuabudu miungu inayoonekana, hilo ni kosa kubwa, imani inajengeka kwa kusikia Neno la Mungu.

Basi Musa aligeuka na kushuka na yale mawe mawili ya bluu yaliyoandikwa pande zote mbili. Alipoona watu wakicheza na kumwabubu yule ndama wa dhahabu, kwa hasira alizitupa zile mbao mbili, akazivunja chini ya mlima. Kisha akatwaa yule ndama wa dhahabu na kumsaga, na unga na mavumbi yake akanyunyiza kwenye maji, na kuwanywesha wana wa Israeli. Musa akamwambia Haruni, “Watu hawa wamekufanyia nini hata ukaleta dhambi hii kuu juu yao”. Haruni hakuwa na jibu la maana bali aliomba hasira za Musa zitulie, na kujitoa kwenye hatia akisema “unajua watu hawa, ya kuwa wamejielekeza kwa mabaya”. Akamweleza yaliyotokea akijitetea kwamba walimpa dhahabu naye “akaitupa ndani ya moto, akatoka ndama huyu”. Sanamu haiwezi kutokea bila kufinyangwa na mtu! Musa akauliza wale walio upande wa Mungu wakae karibu naye, na wana wa Lawi wakawa tayari kukaa upande wake. Siku ile walianguka watu 3000 kwa upanga kutokana na dhambi hii.

Ndama wa dhahabu yawezekana aliwakilisha miungu ya Misri. Fahali wa Apis aliabudiwa huko Memphis, mungu wa uhai. Hathor, mungu wa kike wa ng’ombe, aliabudiwa huko Thebes akiwa mungu wa kike wa uzazi, uzuri, upendo, na shangwe. Katika Kutoka 32 watu “wakainuka kucheza” ambayo ilikuwa na hisia



za wazi za tamaa mbaya na inaweza kulinganishwa na Hathor. Haruni, kiongozi wao wa kiroho, alikubali maombi yao na kuhalalisha ibada yao akatangaza “karamu ya Bwana.” Ibada hiyo iliyochanganyika ilimfanya Mungu kuwakana Waebrania na kumwambia Musa “watu wako.” Lakini Mungu anapokataa watu waliochagua ndama badala ya Yeye, Musa anaingilia kati na kuomba kwamba jina lake lifutwe katika kitabu cha uzima. Upendo wa Musa kwa watu wake ulikuwa mkubwa sana hivi kwamba alitoa uhai wake kwa ajili yao. Lakini kuna kifo kimoja tu cha mbadala kinachokubalika kwa Mungu nacho ni kifo cha MwanaweYesu. Je, umejaribu maishani mwako kuupatanisha ulimwengu na mazoea yake na ibada yako kwa Mungu? Hapa tunaona matokeo ya hatua hiyo. Mungu angekuwa na watu waaminifu kwake, na Yeye tu, hata mbingu zianguke kungekuw ana tofauti. Musa alikuwa hana ubinafsi, alijitoa mhanga apotee, bali watu wengine waokoke. Ninaamini BWANA aliona Musa ana upendo wa kweli. Hakika tabia ya Kristo itakapoonyeshwa mioyoni mwetu kikamilifu ndani yetu, ndipo atakuja kutudai sisi kama watu Wake,

Asubuhi yake Musa aliwaambia watu kuwa wametenda dhambi kuu, naye atakwenda kwa BWANA na kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi yao…Naye akamweleza tena BWANA awasamehe dhambi yao “na kama sivyo, unifute nakusihi, katika kitabu chako ulichoandika”. Musa alikuwa mfano wa Yesu kwa jambo hili. Ndipo Bwana akamwambia Musa yule anayetenda dhambi ndiye atakayefutwa katika kitabu Chake, na akamwambia Musa awaongoze hawa watu mpaka Kanaani, na malaika wake atamtangulia. Hata leo tunaambiwa kuhusu vitabu vitatu: kitabu cha uzima, kitabu cha kumbukumbu, na kitabu cha Hukumu. “BWANA akawapiga hao watu, kwa walivyoifanya ile ndama ambayo Haruni aliifanya”. Utii, unyenyekevu, kujutia dhambi, kutubu na kugeuza njia zetu ni muhimu kwa binadamu wote tukipotoka dhambini.

Hapa ndipo Walawi walichaguliwa watumike kwa kazi ya ukuhani. Watoto wa kiume wa Haruni, Nadabu, Abihu, Eleazari na Ithamari. Musa alizungumza na Mungu uso kwa uso, kama vile mtu anavyozungumza na rafiki. Hajatokea nabii kama Musa aliyemjua Mungu uso kwa uso. Hii haina maana kwamba aliuona uso wa Mungu, bali alikuwa karibu sana na Mungu kiasi kwamba walizungumza kama rafiki wapendwa wanavyofanya. Walikuwa karibu sana hata Musa akatamani sana aone uso wa Mungu. BWANA akamwahidi kuwa “uso Wangu utakwenda pamoja nawe, Nami nitakupa raha…umepata neema mbele Zangu Nami nakujua jina lako… nitapitisha wema Wangu wote mbele yako, Nami nitalitangaza Jina la Bwana mbele yako, huwezi kuniona uso Wangu, maana mwanadamu hataniona

akaishi… utaniona nyuma Yangu, bali uso Wangu hautaonekana”. Musa akataka kujua hili litatokeaje, na BWANA alimwambia apande Sinai Naye ‘atajionyesha’ kwake. Musa alipanda mlimani akiwa amebeba mbao mbili zingine alizochonga mwenyewe, maana zile za kwanza zilivunjika. Musa alipoona yote na kusikia BWANA akizungumza, alipigwa na butwaa wala hakushughulika tena kumwangalia bali akasujudu mbele Zake, yaani uso wake ukagusa nchi.

Watoto na watu wengi leo wangependa kumwona Mungu uso kwa uso, na ni jambo jema, bali kwa sasa hatuwezi, lakini kama tukiwa wema na kumpenda Mungu, siku moja tutamwona uso Wake. Uso kwa uso hakika, pale pale furaha! Sasa ni muhimu tujue kwamba Mwenyezi ni Mwenye rehema, kusamehe, mpole na mwenye kujaa neema na Kweli”. Mtume Yohana anasema, “Mungu ni upendo”, hivyo tunaweza kumwamini kabisa, japo hatumwoni, ila tunamhisi Yu karibu yetu na tunazungumza Naye kwa maombi kila siku tunapoamka, tunapolala, na katikati ya siku. Maisha yetu haya duniani yana maana tu pale tunapojitayarisha ili tuweze kuishi naye milele, ili liwe lengo letu la kwanza kujitayarisha kitabia ili tuishi na Mungu milele. Ile tu kukaa karibu Yake, kumshika mkono, na kuzungumza Naye hata kumkumbatia, tutaona shida zetu zote hapa duniani ni mbilikimo kwa yale mazuri ya milele aliyo nayo kwetu. “Macho hayajaona, wala masikio hayajasikia” yale ambayo Mungu amemtayarishia binadamu. Roho zetu kunawiri kwa burudiko, magumu yote yatakuwa yamepita. Mungu ametutayarishia mambo mema na makubwa mno, mpendwa mtoto, au mtu mzima, usikose kuwepo pale chini ya mti wa uzima mbinguni. Hebu liwe lengo lako na ombi lako, usiku na mchana, kumpenda Mungu. Anza kumwomba Mungu akupatie tabia ya mbinguni, maana kule kama unapenda kupigana, wizi, ukaidi, uvivu au maovu yoyote, utawasumbua wengine. Na hata kama utalazimishwa kwenda, hutaona raha, maana utataka kusema uongo au kumchukia mtu, na hivyo kule havipo. Hata hivyo Mungu akikaribiana na dhambi tu, dhambi huteketea kwani Mungu ni moto ulao dhambi. Hiyo ni sifa Yake. Mwovu ataanza kuteketea mbele Zake bila hata kuguswa na Mungu. Tabia na watu ndiyo vitu pekee tukavyobeba au kwenda navyo mbinguni na sio vitu.

Katika Mlima Horebu, Mungu alikuwa ameanzisha agano na watu Wake. Mungu, kwa upendo wake, aliwachagua Israeli kwa tendo la neema, kama vile katika maagano ya awali yaliyofanywa na wazee wa ukoo. Mungu alikuwa tayari amewakomboa Israeli kutoka Misri na sasa agano Lake pale Sinai linakuwa ni mwendelezo wa tendo hilo la ukombozi. Kuna masharti kwa uhusiano huu wa agano. “Sasa, basi, ikiwa mtaitii sauti Yangu kweli kweli, na kulishika agano Langu, hapo ndipo mtakuwa tunu Kwangu” (Kutoka 19:5). Kufikia wakati huu Israeli walikuwa wamejionea matendo ya pekee ya Mungu ya ukombozi. Sasa Israeli walipaswa kuchagua kwenda peke yao, au kuchagua kuwa watiifu kwa Mungu na kumfuata popote Alipowaongoza? Hapa katika sura hii walionekana wakitenda huduma ya mdomo, maana zilipita wiki 6 tu nao wakajisahau. Je, ni jinsi gani kwetu leo-- Je, tunamtolea Mungu huduma ya mdomo kama watu Wake, na kisha kulalamika na kujaribu kuendelea na maisha yetu bila Yeye? Au Je, tutajibu kama Israeli, “Yote aliyoyasema BWANA tutayafanya?” na tusifanye ( Kutoka 19:8 ). Mungu anajitambulisho hapa kwa Mungu Mwenye Wivu. Ilikuwa shauku ya Mungu kule Sinai na pia leo kuwa na uhusiano wa ndani zaidi,ndani kabisa zaidi, pamoja na watu Wake aliowaumba. Tunaye Mungu

anayesamehe na kuanza tena safari pamoja nasi. Haijalishi dhambi ni mbaya kiasi gani, mara tunapoiungama na kuiacha, Mungu hutusamehe (1 Yohana 1:8, 9). Kwa hiyo tusimruhusu Shetani atusumbue kwa kuileta dhambi kwenye kumbukumbu zetu na kutuambia kwamba hatujasamehewa. Huo ni uwongo, na yeye ni mtaalamu katika hilo.

Musa alipenda sana kupata neema ya  kumwona Mungu uso kwa uso na akamwomba hilo. Akajibiwa "umepata neema machoni Pangu, Nami nakujua kwa jina lako."  Musa akasema "Nionyeshe utukufu wako." Hakuna mwanadamu aliyeanguka dhambini awezaye kusimama mbele za Mungu uso kwa uso, lakini kule kuheshimiana na usafi wa moyo wa Musa kwa wakati huu vilimleta kiumbe huyu na Muumba Wake pamoja. Je! unataka kuhisi uwepo wa karibu wa Mungu katika maisha yako leo? Weka mbali dhambi zote zinazoweza kukutenganisha Naye na umwombe ajidhihirishe katika maisha yako. Mungu yule yule aliyepita mbele ya Musa akiwa amefichwa kwenye ufa wa mwamba anaweza kujidhihirisha kwako. Kwani ni Yesu yule yule Mwenye neema aliyekuja kukuokoa kutoka kwenye dhambi zako.

*Naam Ingekuwa vema kwa wazee na vijana kutafakari Maneno hayo ya Maandiko yanayoonyesha jinsi mahali palipotiwa alama ya uwepo wa pekee kwa MUNGU panavyopaswa kuzingatiwa. "Vua viatu vyako miguuni mwako," Alimwamuru Musa kwenye kichaka kinachowaka moto, "kwa kuwa mahali hapo uilipo simama ni ardhi takatifu." Yakobo, baada ya kuona maono ya malaika, akasema, "Bwana Yuko mahali hapa; na sikuijua .... Hapa si mahali pengine bali nyumba ya MUNGU, na hili ndilo lango la mbinguni. "

---

Je, watu walikuwa waaminifu kwa Mungu wakati Musa alipoenda mlimani? Kwa nini walifanya uasi wiki sita tu toka waliposema watatunza amri zote? Musa alifanyaje alipoona uasi waliofanya? Je, tunajifunza nini hapa? Urafiki wa Musa na Mungu ulikuwaje? Je, Haruni alionesha uongozi wa namna gani? Lazima tujitenge na ulimwengu, lakini pia watu waweze kutufikia-Jadili sentesi hii ya kuwepo duniani pasipo kuwa wa dunia.

**SIKU YA 39**
**( Februari 8)**

# Musa Aenda Tena Mlimani

**- Kutoka 34 na 35**

Musa aliposhuka tena kutoka mlimani baada kuandikiwa amri kumi kwenye mbao alizozichonga, akiwa amekaa siku 40, uso wake uling'aa mpaka kaka yake Haruni akaogopa kumsogelea. Ilibidi ajifunike uso wake alipokuwa akizungumza na watu. Kwa mara ya pili, Mungu aliandika Amri Kumi kwa kidole Chake kwenye mbao za mawe. Sheria ambayo Mungu aliisoma binafsi, na kusikika kwa wanadamu (Kutoka 20:1-2), na kuiandika mara mbili juu ya jiwe hivyo lazima ichukuliwe kwa uzito kwa sababu bila shaka Yeye anaichukulia kwa uzito. Tutahukumiwa na hii "sheria iletayo uhuru" (Yakobo 2:12). Kuvunja amri moja ni kuvunja zote kumi maana ni kitu kimoja. (Yakobo 2:10). Alisikia Mungu akisema, "Bwana, Mungu mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na Kweli; Mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, Mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi." Musa aliposikia hivi alisujudu, na kumwomba BWANA aende, "kati yao, maana ni watu wenye shingo ngumu, ukasamehe uovu wetu na dhambi yetu, ukatutwae tuwe urithi Wako." Musa alimwakilisha Kristo kwa kuwaombea wana wa Israeli msamaha kwa uovu wao. Akawaambia Waisraeli wajihadhari wasije wakaabudu miungu mingine kwa maana Yeye BWANA ni "Mungu mwenye wivu kwa watu Wake". Wivu huu ni mtakatifu, maana Yeye Ndiye aliyetuumba, hivyo ni Yeye tu Mwenye haki ya kuwa na wivu, au kuangamiza alichokiumba. Hata sisi watoto, tukiamua hatuheshimu au kuwasaidia wazazi wetu, eti tunasaidia watu wengine, kuchota maji, kufua, kuwapa mahitaji yao, na kutelekeza wazazi, je, hawatakuwa na wivu?



Musa aliposhuka, watu walikuwa tayari kujenga hekalu kama walivyoagizwa. Bali walijaribiwa ili kuona kama wanajali mambo ya kiroho au ya Mungu kwa kutoa sadaka zitakazotumika kujenga hekalu. Watu walikuja na hivi vitu toka utumwani Misri. Mungu hakuwalazimisha japo Ndiye mpaji, bali aliwaambia ni sadaka ya hiari ya moyo "yeyote ambaye moyo wake unamtuma…". Mpaka hapa walikuwa ni watu wa kupewa vitu, ila sasa Mungu alitaka nao watoe. Walikuwa tayari kutoa, na wakatoa kwa moyo wa furaha, labda wachache tu walinung'unika kutoa. Kutoa ni bora

kuliko kupokea, kutoa ni tabia ya mbinguni, kusaidia wenye mahitaji na kugawana na wenzako kidogo ulicho nacho. Usile na mtoto mwingine anakutazama na tena ana njaa, au una penseli mbili unakaa nazo na mwingine hana fedha ya kununua hata moja. Lilikuwa jambo la furaha kuona watu wakileta vitu. Wakaja kila mtu ambaye moyo wake ulimhimiza. Walileta dhahabu, nyuzi za kitani, fedha, wakaleta sadaka ya kumpa Bwana mchana na usiku; mpaka wale waliokuwa wanapokea na kuweka kwenye ghala wakasema, "vimetosha", waache kuleta sadaka! Je, hili si lingekuwa jambo zuri kwenye kanisa lako leo, watu kutoa mpaka mbiu ya kuwazuia ipigwe "msilete tena, sadaka kwa kazi ya Bwana maana imejaa na kufurika". Hii inaonesha walikuwa hawana uchoyo au ubinafsi, basi ni nani tumpe mali zetu kama si yule anayetupatia kila kitu? Leo watu wanajenga makanisa au nyumba za ibada kila mahali, na tuombe isichukue miaka mingi kwisha! Na tujaribu kuepuka kujenga mahali pa kuabudia kwa madeni, kadri tunavyoweza.

BWANA alipowaambia watu kutoa sadaka, alitaka pia watoe muda wao, na kujitolea wao wenyewe kusaidia kazi ya kujenga hema ya kukutania. "Kila mtu kati yenu aliye na moyo wa hekima na aje, na kuyafanya hayo yote ambayo BWANA ameyaagiza, yaani hiyo maskani na hema Yake, … wanawake walio na hekima nao wakasokota kwa mikono yao nyuzi na kuzileta
'kwa moyo wa kupenda au hiari moyo'".

Ndipo Musa akawaambia Waisraeli, "BWANA amemwita kwa jina lake Bezaleli mwana wa Uri, mwana wa Huri, wa kabila la Yuda; Naye amemjaza Roho ya Mungu, katika hekima na akili, na ujuzi na kazi ya ustadi wa kila aina; na kuvumbua kazi za werevu na kufanya kazi ya dhahabu, fedha… na kukata vito vya kutilia, na kuchora miti, atumike katika kazi ya werevu wa kila aina" pia apate "kufundisha" wengine kufahamu ustadi, ufahamu, uvumbuzi na hekima hii. Msaidizi wake alitajwa pia, "Oholiabu mwana wa Ahisamaki wa kabila la Dani. Amewajaza watu hao akili moyoni, ili watumike katika kazi ya kila aina, iwe ya kutia taraza, kuchora mawe, kufuma nguo na zingine za kuvumbua zinazohitaji kusugua kichwa. Musa aliwaita vijana hawa, na wengine ambao walikuwa tayari kusaidia kazi hii kubwa. Bila shaka Bezaleli alishughulikia mwenyewe zile samani za Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu. Alipata kazi ya ajabu, kushughulika kutengeneza vifaa vitakatifu kama "kiti cha rehema". Vitu hivi vilitumia dhahabu nyingi! Kisha wakatengeneza na mavazi ya makuhani

Kama kuna watu waliopata mshangao, basi ni Bazaleli na Oholiabu, maana Mungu aliwaita kwa majina yao bila hata kutegemea. Na tena hapa inasemwa wazi kwa mara ya kwanza kwamba Aliwajaza na Roho Mtakatifu, kwa majina ya siku hizi fani hizi ni mainjinia, watu wa kuchora ramani, na watu wa kupamba (Engineer, interior decoration, graphic design, architecturer) Pengine wengi hawakuwajua vijana hawa, lakini hili linatuonesha kuwa Mungu anamjua kila mtu na roho zetu pia na hata yale tunayoweza kuyafanya kuliko hata sisi wenyewe tunavyojua. Jiulize leo "Mungu anajua" mambo gani kukuhusu?"

*Unyenyekevu wa Sulemani wakati alipoanza kubeba mizigo ya serikali, alipokiri mbele za MUNGU, “Mimi ni mtoto mdogo tu” (1 Wafalme 3:7), upendo wake wa ajabu kwa MUNGU, kicho na heshima yake kuu kwa mambo ya Bwana, kutojiamini kwake ndani ya nafsi yake, na kumwinua kwake Muumba wa yote asiye na kikomo—mienendo yote hii ya tabia, zinazostahili kuigwa sana, zilifichuliwa wakati huduma ya ibada zilizounganishwa na ukamilishaji wa ujenzi wa hekalu, wakati wa maombi yake ya kuweka wakfu hekalu alipiga magoti katika mkao/nafasi ya unyenyekevu ya mwombaji. Wafuasi wa Kristo leo wanapaswa kujilinda dhidi ya mwelekeo wa kupoteza roho ya staha na hofu ya kimungu. Maandiko huwafundisha wanadamu jinsi wanavyopaswa kumwendea/kumsogelea Muumba wao—kwa unyenyekevu na kicho, kupitia imani katika Mpatanishi wa Kiungu/Mbingu.

---

Somo gani umejifunza leo? Kwa nini kutoa ni bora kuliko kupokea? Musa alijuaje kuwa Bezaleli ana karama ya ustadi na taaluma ya ujenzi? Nani alikuwa msaidizi wa Bezaleli? Kwa nini Bezaleli alifundisha? Ni wapi kwa mara ya kwanza kwenye Biblia wamesema Mungu amemjaza mtu na Roho Mtakatifu?

**SIKU YA 40**
**( Februari 9)**

# Sababu za Kuwa na Patakatifu

**- Kutoka 25, Mambo ya Walawi 16 na 22**

Mungu aliagiza kujengwa kwa hema au hekalu la kukutania ili aweze kukaa na watu Wake. Patakatifu palikuwa pia mahali pa kuungama dhambi na kusamehewa. Mungu alikuwa ametoa njia ya kusafisha uovu wetu kwenye madhabahu. Hema hii ilikuwa ni kielelezo cha hema halisi iliyo mbinguni ikielezea mpango wa wokovu ambao wangeuona kwa macho (Picha ya wokovu) (Waebrania 2, 3, 4,8, 9,10). Tunaambiwa twende kwake kwa ujasiri kupitia njia hii. Pia mpango huu ungewasaidia wasiabudu sanamu bali waendelee kujifunza kweli kwamba Mungu haonekani kwa macho yetu ya dhambi kwa wakati huu. Patakatifu pangekuwa ni hema ambayo "Mungu angeishi na watu Wake, au watu wangekutana na Mungu". Hema ilikaa katikati ya kambi ya Waisraeli na karibu na nyumba ya Musa. Hema ilikuwa na mihimili na mapazia ya rangi nzuri kuizunguka.

Uwepo wa Mungu ni kila mahali lakini anao mji Wake kule mbinguni na hekalu lile Takatifu. Kama binadamu hatujui sana anavyoonekana kwa macho, tunaambiwa ni Roho katika Yohana 4:24 na 1 Wafalme 8:27. Biblia inatuambia wazi kwamba mbinguni kuna hema na mbinguni ni mahali halisi. Kuna mengi magumu ambayo



hatuyaelewi wala kuweza kuyafikiria kwa bongo zetu. Ni kwamba imetupasa tuiamini Biblia japo hatuwezi kujua mengi kwa ndani, lakini tujifunze kumwamini Mungu na yale tusiyoyaelewa, baadae kwa wakati Wake atatufunulia. Katika kitabu cha Waebrania 10:25 tunashauriwa tusiache kwenda kwenye ibada na Yesu alikuwa na desturi hiyo kila wiki Luka 4:16. Tujitahidi tusichelewe kwenda kwenye ibada, au kufika kule na kupiga kelele, kutafuna tafuna chakula au kucheza. Nyumba ya Mungu ni mahali Patakatifu pa kukutana Naye.

Mpango wa wokovu umejikita kwenye kafara. Yesu alikuja na kuishi na watu, akafa na kufufuka ili tuwe na uzima wa milele. Hata leo Mungu anataka tutoe miili yetu kuwa dhabihu Iliyo hai. Mpendwa mtoto, kutii ni kafara au sadaka bora kuliko dhabihu. Biblia inatuonesha kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu. Kristo Ndiye kuhani wetu na mhukumu wetu pale hekaluni mbinguni.

Katika kitabu cha Danieli 7:10 inasema, "Maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele Zake, hukumu ikawekwa na vitabu vikafunuliwa". Hekalu kwa Wayahudi lilikuwa na maana kubwa katika nchi kwa uchumi au hata utawala wa nchi. Baada ya muda walisahau kwamba lina maana gani. Walisahau kuwa linahusiana na Mungu na mpango wa wokovu.

Baada ya Kristo kufa msalabani (Mathayo 27:50, 51) na kwenda mbinguni, hekalu la duniani halisimami tena, lakini bado Mungu anataka kukaa na watu Wake kupitia Roho Mtakatifu. Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu. Tunapaswa tuitunze vizuri kwa usafi, kwa kutojichafua kwa mawazo, matendo au maneno yasiyo safi. Vitu kama pombe, sigara, mawazo mabaya na matendo ya uovu yanaharibu hekalu la Mungu.

Japo tu watoto, hili tutaendelea kulielewa kadiri tunavyokua. Ni kweli tunaokolewa kwa Kifo cha Yesu msalabani, na sio kwa matendo bali tunapomjua Yesu matendo yetu na tabia zetu zinabadilishwa tufanane Naye. La muhimu kuhusu hekalu ni kwamba hata leo Mungu anataka kukaa pamoja nasi ndani ya mioyo yetu, na tulinde njia za kuingia mioyoni mwetu, yaani tunachoona, na tunachosikia, tunachonusa, na tunachogusa. Na njia Yake iko katika Patakatifu (Zaburi 77:13)

Kitabu cha Mambo ya Walawi kinatuambia kulikuwa na sikukuu mbalimbali kando ya hii kubwa ya siku ya upatanisho, nazo ni siku ya Sabato, sikukuu ya Pasaka iliyo na mikate isiyotiwa chachu, sikukuu ya vibanda au makambi, sikukuu ya tarumbeta na sikukuu ya majuma ambayo baadaye iliitwa Pentekoste.
Yesu hatuiti kwa ajili ya kuomba tu kanisani au kwenye hekalu, bali anatuita pia kuhudumia mahitaji ya wale wanaotuzunguka. Hatuweza kugusa mbingu, bila ya kugusa watu. "Kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia" (Mathayo 25:35, 36). Tunapaswa kuishi maisha yenye sura mbili – maisha ya mawazo na matendo, na maisha ya maombi ya kimya na kazi inayofanywa kwa juhudi. Tumepokea upendo mwingi sana kutoka kwa Mwokozi wetu; na tuna fursa ya kushiriki upendo huo na marafiki, majirani, hata watu tusiowafahamu wenye uhitaji. Muulize Mungu

katika maombi namna bora ya kuwafikia wengine. Tanguliza maombi mengi ya faragha; kwani hekima kubwa inahitajika ili kuelewa sayansi ya kuokoa roho. Kabla ya kuwasiliana na watu, wasiliana na Kristo. Pata maandalizi ya kuhudumia watu kutoka katika kiti cha enzi cha neema ya kimbingu. Hapa kuna baadhi ya njia unazoweza kutumia kusaidia wengine. Chagua njia yo yote utakayoona inakidhi mahitaji ya wale unaokwenda kuwahudumia, na jisikie huru kuongeza mawazo yako.

- Mpatie mwanafunzi fedha ya "chakula."
- Kusanya nguo kwa ajili ya wahitaji.
- Gawa vijarida na vijuzuu kwa watu.
- Msomee mzee kitabu.
- Tembelea makazi ya watoto yatima

Umaalumu wa maagizo katika Mambo ya Walawi ni ukumbusho kwamba Mungu anapenda utaratibu, mpangilio, muundo, na usahihi. Mungu pia ni mpenda uzuri na usanii! Wale ambao wamejaliwa katika sanaa hakika hupata faraja na furaha katika sura hizi. Mungu Mwenyewe alitoa talanta ya usanii kwa Bezaleli na Oholiabu. Kutumia karama zao katika kujenga hema la kukutania kulimletea heshima Mungu ambaye walimtumikia. Watu walitoa kwa mradi wa ujenzi kwa ukarimu wa shangwe hivi kwamba hatimaye amri ikaja, "Msilete tena!" Si mara nyingi leo tunasikia habari za uchangishaji fedha kwa ajili ya mradi maalum wa utume unaoleta rasilimali nyingi kiasi kwamba kiongozi anasema, Inatosha! Usichangie zaidi! Hakika kutoa ni bora kuliko kupokea. Nguvu, ubunifu, ushupavu, na shauku ya Israeli ya kale ya kujenga kwa pamoja jumba la ibada ambalo lingemheshimu Mungu bado vinahitajika kwa watu wa Mungu leo. Haijalishi kama sisi tu walinzi au wabunifu tunapomtumikia na kumwabudu Bwana kwa talanta zetu.

*Ndipo Sulemani akapiga magoti juu ya jukwaa la shaba, na katika usikivu wa watu wote alitoa ombi la kuweka wakfu hekalu. Akiinua mikono yake mbinguni, huku kutaniko likiwa limeinama kifudifudi (sura zao zikiwa kwenye sakafu), mfalme alisihi: "Bwana, MUNGU wa Israeli, hakuna MUNGU kama Wewe mbinguni, wala duniani; ushikaye maagano, na kuwarehemu watumishi Wako, waendao mbele Zako kwa mioyo yao yote.


---

Je, mbinguni patakuwa na hekalu? Kwa vile miili yetu ni hekalu la Roho wa Mungu tunapaswa tusifanyeje? Kuna umuhimu gani kwenda katika ibada au kanisani? Nini maana ya Takatifu? Kwa nini hekulu ni Takatifu?

**SIKU YA 41**
**( Februari 10)**

# Kuwaweka Wakfu Makuhani na Mavazi yao Kwa Uzuri na Utukufu wa Mungu

**- Kutoka 28, 27, 39 na 28**



Bezaleli, Oholiabu na wasaidizi wote waliotaka kumfanyia kazi BWANA kwa sadaka ya talanta na muda wao waliendelea kujenga. Wengine kuchambua nyuzi mbali mbali, au ngozi. Wengine kuweka rangi kwenye kitani. Wengine walikuwa wakitazama na kuuliza maswali ya kinachoendelea huku wengine wakisaidia. Huenda Musa alijibu maswali mengi yahusuyo mpango wa wokovu wakati ujenzi ukiendelea. Hakukuwa na magazeti au redio ila habari za hekalu na ujenzi wake zilienea kwa kile kilichokuwa kinaendelea.

Katika mahali patakatifu kama hapa, kazi inabidi ifanywe na utaratibu, mipango na kicho. Kupiga makelele ovyo, mazungumzo yasiyofaa au hata mawazo mabaya vinaleta hatari. Na hata leo tunapoenda kanisani kwenye nyumba ya ibada, tuepuke kupiga kelele, na kujifanyia mambo yetu. Kanisa ni chombo kiteule kitakatifu, kilichopewa utume wa kuhubiri habari njema za Mungu na ufalme Wake unaokuja karibuni. Mungu anatoa kipaumbele kwa kanisa Lake. Tunapokuwa kanisani yatupasa tuwe kimya, na tuje tumevaa kwa heshima. Kuchelewa kanisani na kuwa

na mawazo mengine wakati wa ibada ni dhambi. Kuna kitabu kinaitwa Shuhuda kwa Kanisa Gombo la 5 sura ya 55 imeelezea vizuri mwenendo tunaopasa kuwa nao kanisani, kama huna kitabu hiki tuandikie tukutumie nakala ya kiswahili, ila ya kingereza ipo bure mtandaoni. Ilimchukua Injinia au mhandisi Bezaleli miezi sita kufanya shuguli ya Patakatifu. Alikuwa amefanya kazi njema, na hata kushona nguo za makuhani. Pengine Musa alimpongeza kwa kazi njema aliyofanya jangwani kwa ajili ya patakatifu. Waliweka zile fanicha, Musa aliweka zile mbao mbili za Amri Kumi mwenyewe. Kila kitu kikawa kwenye mpangilio na ghafla watu wakiendelea kutazama waliona "wingu lililokuwa na utukufu wa Mungu". Watu wakafurahi walipojua kwamba Mungu alikuwa pamoja nao na amependezwa na kazi waliyoifanya. Furaha ya Mungu ndiyo nguvu yetu. Usiku Hekalu au hema la kukutania likaonekana linang'aa kwa ule mwanga wa moto. Wingu lile lilitoa joto la jangwa pia na moto vilipunguza baridi ya jangwani. Mungu ni mpaji wa mahitaji ya watu Wake yote. Na yeyote aliyekuwa ana huzuni, au shida akiliona wingu alifarijika. Walikuwa na "taa na kiyoyozi wasivyolipia".

Baada ya wiki chache Haruni na watoto wake wanne wa kiume walifanyiwa huduma ya kuwekwa wakfu ili watumike kwenye hekalu. Kila mtu alialikwa, wakaona watu sita: Musa, Haruni, Nadabu, Abihu, Eleazari na Ithamari wakiingia wakiwa wamevaa kaptura. Musa akachukua maji na kuwaosha wale watano, kuwatayarisha kwa huduma takatifu mbele ya Bwana kwenye hema. Kisha Musa akamvika Haruni nguo zake, zilizoonekana maridadi sana kwa mshono na rangi ya bluu, zambarau, nyekundu na dhahabu kama vile pazia za hekalu zilivyokuwa. Bluu ikisimamia Sheria ya Mungu, nyekundu rangi ya dhambi, zambarau mchanganyiko wa bluu na nyekundu ikisimamia rehema, na manjano ya dhahabu ikisimamia haki. Kwenye kifua chake Haruni alivalishwa Naivera ikiwa na vito vya mawe 12 yaliyong'aa na kuandikwa majina ya makabila ya Israeli. Kwenye mabega yake kulikuwa na mawe mawili ambayo kila moja lilikuwa na majina ya makabila sita ya Israeli yakimkumbusha kwamba anabeba mizigo au dhambi za Waisraeli mabegani na moyoni mwake. Musa akaweka ukosi wa rangi ya dhahabu kwenye kichwa cha Haruni wenye maneno "Mtakatifu kwa Bwana". Haruni alipaswa kuwakilisha utakatifu. Bila ya kuelezea kila kipande cha vazi, kila kitu kilimwakilisha Kristo. Je, mavazi yetu yanawakilisha nani? Mavazi haya hayakukusudiwa kuleta umakini na utukufu kwa wale walioyavaa, lakini badala yake kuleta utukufu kwa Mungu. Je, viongozi wa kidini leo lazima wavae mavazi ya kifahari, yaliyopambwa kwa dhahabu na vito kama siku zile? Vazi zuri kupita yote, ni vazi la haki ya Kristo. Haruni pia alikuwa na mawe mawili, kushoto na kulia kwenye mabega yaliyoitwa Urimu na Thumimu, ambayo yalikuwa herufi za alfabeti ya Kiebrania ya kwanza na ya mwisho. Haya yalitumika kutoa majibu kwa mashauri, endapo jiwe la kulia kwa bega likitoa mwanga jambo hilo limekubaliwa na Mungu. Likiwa halijakubaliwa basi jiwe la kushoto litakuwa na kivuli. Nguo za Haruni pia zilishonewa njuga za dhahabu ili aingiapo na atokapo sauti yake itasikika, endapo atakuja kwenye hema bila kuvaa ile nguo, angekufa.

Haya yakiendelea Nadabu, Abihu, Eliezari na Ithamari walikuwa wamesimama wakiangalia na mwishowe ikawa zamu yao kuvikwa nguo. Hazikuwa kama za baba yao bali zilikuwa nzuri na za utukufu.

Kisha akaletwa ng'ombe kwao wakiwa wamesimama na Haruni na vijana wake wakaweka mikono yao juu ya kichwa chake wakiungama dhambi zao, na Musa akamchinja mnyama huyo na kunyunyiza damu kwenye madhabahu. Kisha kondoo aliletwa na Haruni na watoto wake wakaweka mikono yao juu ya kichwa chake na akachinjwa na damu yake ikanyunyuziwa kwenye madhabahu. Kisha kondoo mwingine wa kujiweka wakfu akaletwa na makuhani hawa watano wakaweka mikono yao kwa mnyama huyo wakiwakilisha "kuweka dhambi zao". Ila safari hii badala ya kunyunyiza damu yake kwenye madhabahu, Musa aliweka damu hii kwenye ncha ya sikio, kidole gumba cha mkono na kidole kikubwa cha mkono wa kulia wa Haruni. Kisha akaenda kwa wale vijana wanne na kufanya vile vile kwenye sikio, kidole gumba na kidole cha mguu wa kulia. Damu kwenye sikio la kulia kumaanisha wasisikie uovu wowote, bali waweke mawazo yao kuwa safi na wakfu. Damu kwenye kidole gumba iliwakilisha kutumia mikono yao kufanya mambo matakatifu yasiyo na uovu, kusaidia masikini, yatima na wajane, na kujenga ufalme wa Mungu. Damu kwenye kidole kikubwa cha mkono wa kulia ilisimamia kwenda katika njia za haki. Kufuata Amri cha Mungu, na kutotangatanga katika uovu ambapo Mungu hakutaka waende.

Kwa kifupi, huduma hii ilikuwa ya kuwaweka wakfu au utakatifu kwa Mungu na kazi Yake Takatifu aliyotaka waifanye. Hata sisi leo tunapaswa kuwekwa wakfu na damu ya Yesu, masikio, vidole na miguu yetu ili tuwaze yaliyo mema na Matakatifu, tufanye mema na twende katika njia za haki za Mwenyezi. Hata siku hizi watumishi wa Mungu na nyumba ya ibada huwekwa wakfu. Watumishi wa Mungu wanapaswa kuheshimiwa kwa vile wanamwakilisha Mungu. Na hekalu linawakilisha nyumba ya Mungu hapa duniani, si mahali pa kupiga usingizi kama tupo hotelini au kusengenya watu na kuleta "mazungumzo baada ya habari". Ni mahali pa kutulia na kuabudu. Ombi: Baba nisaidie kujua kwamba sijafika nyumbani bado, na kwamba mimi ni mgeni na msafiri hapa duniani. Unikomboe kutoka katika udanganyifu wa kutembea njia pana wakati nakutumikia. Naomba uniweke wakfu kwa kazi Yako na kunisaidia kuwa na nia ya mbinguni, iliyo yenye manufaa Kwako na wanadamu pia.

*Mmepewa akili ili muweze kuelewa jinsi ya kufanya kazi. Mmepewa macho ili muweze kuwa makini katika kuzitambua fursa mlizopewa na MUNGU. Masikio yenu yasikilize maagizo ya MUNGU. Magoti yenu yanapaswa kupigwa mara tatu kwa siku katika maombi yanayoyotoka moyoni. Miguu yenu na itembee katika njia ya amri za MUNGU.

---

Ni watoto gani wa Haruni waliwekwa wakfu? Damu sikioni ilimaanisha nini? Kwa nini ni muhimu tuwaheshimu watumishi wa Mungu? Mambo gani hatupaswi kufanya tukiwa kwenye ibada?

**SIKU YA 42**
**( Februari 11)**

# Huduma za Patakatifu

**- Kutoka 27, 35-40 na Mambo ya Walawi 1 na 8 na Hesabu 10**



Kitabu cha Mambo ya Walawi kinaelezea kwa undani huduma za makuhani na kafara. Pale ambapo watu wangehama kusonga mbele, makuhani wangefunika fanicha/samani zote na kuweka vizuri vitu vyote vya hekalu. Musa angesimama na kusema "Inuka Ee Bwana, adui Zako na watawanyike na wakimbie mbele Zako hao wakuchukiao". Maneno haya yalikuwa mazito kuyasema, hasa ukitilia maanani kwamba kuna Waisraeli waliokuwa maadui za BWANA pia! Kisha walawi wangebeba Sanduku la Agano na hema kuwatangulia watu, na makabila 12 ya Israeli yalifuatia kwa mpangilio nyuma yao. Wingu liliwatangulia, na wakaendelea mbele hivyo kwa miaka 40 jangwani. Walipofika na kusimama mahali walipopiga kambi, Musa alisema "Ee Bwana, uwarudie maelfu kumi na maelfu ya Israeli". Kwa Amri ya Bwana wingu likiondoka walisafiri na kwa amri ya Bwana walipiga kambi lile wingu lilipofika mahali likatulia. Kisha hema ya kukutania ilisimamishwa kwanza, na kuzungushiwa ua wa hema kisha makabila matatu yalikaa kwenye kila upande wa lile hema. Kila mahali ambapo dhabihu ingeteketezwa na Waisraeli, walikumbuka kuwepo kwa Mungu kati yao na kwamba hakuna haja ya kujitengenezea miungu mingine. Waliendelea kumwabudu Mungu katika Roho na Kweli.

Kila asubuhi kuhani angekuja kwenye madhabahu mbele ya hema ili kushugulikia moto kwa kuweka kuni, ili uendelee kuwaka, moto uliwaka saa zote hata wakisafiri.

Mungu aliuwasha mwenyewe ila makuhani waliendelea kuweka kuni. Kila asubuhi na jioni Kuhani alichukua koleo la makaa yanayowaka na kuyaweka kwenye bakuli lenye kamba ya chuma cha kubeba mkononi. Kuhani angeweka uvumba kwenye moto na ukatoa mwanga na moshi wenye harufu ya manukato, kisha akaupeleka Patakatifu, moshi huu uliwakilisha maombi ya watakatifu yanayokwenda juu mbinguni. Asubuhi na jioni kuhani angeleta kafara ya ndama au kondoo na kumchinja na kuchukua damu yake kwenye beseni na kuweka ile kafara kwenye madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa kwa ajili ya Israeli mara mbili kwa siku. Pale tu wanapojitoa kwa Mungu Naye Mungu angewasamehe na kuchukua dhambi zao.

Huduma hii iliwakilisha maana kubwa zaidi kwa kulenga kafara ile halisi itakayoondoa dhambi za ulimwengu, ambayo Mungu angekuja kuitoa miaka elfu inayokuja. Yesu Ndiye Mwana- Kondoo, Yeye Mwana wa Mungu angetoa uhai Wake kwa kusulibiwa msalabani. Waisraeli wengi hawakuelewa hili vizuri kama ilivyo kwetu sisi, maana tunaishi baada ya Kristo kuzaliwa na tunalo Neno la Mungu, yaani, Biblia.

Mara zingine mtu alikuja na sadaka ya binafsi ya mwana-kondoo au ng'ombe. Mnyama huyu ilikuwa lazima awe mkamilifu bila kilema chochote. Hatumpi Mungu wetu mkuu vitu ambavyo tumevichoka, au chakavu na vyenye kasoro. Nafikiri hata rais wako wa nchi au rafiki yako mkubwa huwezi kumpa vitu vyenye kasoro. Mtu huyu ambaye alitaka kumwabudu Mungu kwa kutoa sadaka, alifika mbele ya madhabahu ya sadaka ya kuteketeza na kuweka mikono yake juu ya mnyama, ikawa kama mnyama anamwakilisha, kwamba anapomtoa kwa Mungu, ni Yeye amejitolea. Kisha alimchinja mnyama na kuhani aliweka kuni kwenye madhabahu, wakati mtu huyo amesimama akiangalia mnyama anavyoteketea, na kutoa shukurani Zake kwa Mungu na kushukuru kusamehewa dhambi zake. Yesu alipokuja na kuishi hakuvunja Sheria!

Sadaka zingine zilikuwa za unga wa nafaka wenye mafuta ya mizeituni, chumvi, juisi za zabibu na mboga mboga. Sadaka za amani na ushirika. Sadaka zilikuwa zinateketezwa na kuisha, ila kuna sadaka zingine sehemu zake zilikuwa za makuhani kula kwa kufuata sheria Mungu alizozitoa. Sadaka hizi za kuteketezwa ndizo ambazo Sheria zake ziliisha Yesu alipokufa msalabani na si Amri Kumi. Sheria ya Mungu ni tabia Yake, mbingu na dunia zitapita ila si Neno au Sheria Yake.

Kila siku kuhani alienda Patakatifu na kuweka zile taa saba mafuta. Taa hizi ziliwaka saa zote. Taa zilimwakilisha Yesu Ambaye Ndiye "Nuru ya ulimwengu". Kila Sabato asubuhi kuhani alikuja na mikate mipya wakaiweka badala ya ile iliyotangulia. Makuhani wakisimama hapa waliila ile mikate ya zamani. Mkate ulisimamia Kristo Mkate wa Uzima au Neno la Mungu.

Mungu alimchagua Haruni na vijana wake wanne kuwa makuhani, na wazao wao katika hema hii. Haruni na wana wake walipokuwa madhabahuni hawakuvaa viatu wala soksi. Hii ni kwa vile palikuwa mahali Patakatifu. Mahali pengi duniani watu huvua viatu vyao. Ni Walawi tu ndio waliochaguliwa ukuhani. Haruni na vijana wake wangeingia Patakatifu, bali ni Haruni peke tu au kuhani mkuu ambaye

angeingia Patakatifu pa Patakatifu. Haruni na wanawe “wajitenge wenyewe na vitu vitakatifu vya wana wa Israeli ambayo watanitakasia Mimi, tena kwamba wasilinajisi Jina Langu Takatifu, Mimi Ndimi Bwana”.

Hapo awali Mungu alizungumza kutoka Mlima Sinai na watu Wake. Sasa Mfalme wa mbinguni alikuwa anawasiliana na watu kutoka kwenye jumba Lake jipya lililobebeka (madhabahu ya kukutania). Katika Mambo ya Walawi, jumbe Zake maalum kuhusu ibada na maisha matakatifu zimeandikwa katika Maneno Yake Mwenyewe. Katika moyo wa Torati (vitabu vitano vya Musa), ambao ndio msingi wa Biblia nzima. Mambo ya Walawi ina hotuba ya moja kwa moja ya Mungu kuliko kitabu kingine chochote cha Biblia.

Maagizo ya awali ya Mungu kutoka Patakatifu yanahusu njia za kumkaribia kwa njia ya dhabihu (Walawi 1-7). Kwanza ni sadaka ya kuteketezwa, ambayo tayari inajulikana tangu zamani (Mwa 8:20; 22:13). Dhabihu zilitofautiana kwa gharama yaani mifugo mikubwa hadi wanyama wadogo na hata ndege, jambo ambalo liliwaruhusu hata Waisraeli maskini zaidi kutoa ibada. Katika kila sadaka ya kuteketezwa, dhabihu ilipanda moshi kutoka kwa madhabahu ya Bwana, isipokuwa kwamba ngozi ilikuwa ya kuhani anayehudumu ili kumfidia kwa ajili ya utumishi wake (Mambo ya Walawi 7:8). Hata kuhani hakuweza kula kutoka kwa sadaka ya kuteketezwa.

Sadaka za kuteketezwa ziliwafundisha watu waliotengwa na Mungu kwaajili ya dhambi kwamba wangeweza tu kuja Kwake kupitia dhabihu kamili ya Mwanawe mpendwa, ambaye angejitoa mwenyewe “mara moja tu” (Ebr 7:27; linganisha Yohana 1:29; 3) Hivyo ndivyo Mungu anavyokupenda wewe na mimi, Naye anataka turudi wakati tumetengwa naye!

Kusudi la dhabihu za wanyama, kama sehemu ya kazi za Patakatifu, ilikuwa ni kuonyesha kwa njia ya mfano jinsi dhambi inavyoshughulikiwa. Kwamba kwa kila dhambi ninayofanya, Mtu mkamilifu asiye na hatia lazima afe. Kabla ya kuwazia moyoni juu ya uvumilivu Wake, na asili ya kusamehe, je, kweli unataka kumpigilia Yesu misumari mikononi Mwake?Jamii na kanisa lililo na utaratibu mzuri linahitaji utii na ushirikiano. Musa alifanya kama Mungu alivyomuomba afanye ili pahali Patakatifu pawepo. Watu walifuata nguzo ya mawingu na moto katika safari yao. Ikiwa dhabihu ya wanyama ilikuwa njia ambayo watu wa Agano la Kale walipaswa kuonyesha imani yao katika Mwokozi ajaye, je, ni njia gani sisi tunaoishi baada ya msalaba tunadhihirisha imani katika dhabihu ya Yesu?

Hoja hii mtanziko inajibiwa kwetu leo “Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyomkabidhi ninyi: kwamba Bwana Yesu katika usiku ule aliotolewa alitwaa mkate; na alipokwisha kushukuru, akakimega, akasema, ‘Twaeni, mle; huu ndio mwili Wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho Wangu.’ Vivyo hivyo akatwaa kikombe baada ya kula, akisema, ‘Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu. Fanya hivi, mara nyingi unapokunywa, ndani ukumbusho Wangu.’ Kwa maana kila muulapo mkate huu nakunyweni kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.” 1 Wakorintho 11:23-

Hivi ndivyo ushirika mtakatifu ulivyo muhimu. Yaani ile meza ya Bwana. Ni muhimu kwa wale wanaoishi baada ya msalaba kama vile dhabihu ya wanyama ilivyokuwa kwa wale walioishi kabla ya msalaba. Kwa hivyo, usikose ibada inayofuata ya ushirika mtakatifu wa meza ya Bwana katika kanisa lako la karibu kama umeshabatizwa tayari! Kama hujabatizwa na unaweza kuelewa mafundisho vyema, zungumza na mchungaji wako.

Je! Kwa nini hatuna aina hii ya huduma ya kuwekwa wakfu makuhani kwa kunyunyiza damu katika Agano Jipya? Kwa sababu Yesu sasa ni Kuhani wetu Mkuu, na kila Mkristo ni kuhani (Angalia Waebrania 8:1-2; 1 Pet. 2:9,10). Kwa hiyo tujikumbushe sisi wakristo ni makuhani, tumetengwa na Mungu kwa ajili ya utumishi Wake mtakatifu. Na ni nini anachohitaji kutoka kwetu kama watumishi Wake? Anatuambia hivi: "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuona matendo yenu mema na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni." Yesu anapoinuliwa kwa njia hii, anawavuta watu wote Kwake ili waweze kuokolewa (Yohana 12:32).
Kwa hiyo, kabla Haruni na wanawe hawajaanza huduma yao ya ukuhani, walipaswa kuwekwa wakfu. Musa akawaosha Haruni na wanawe. Hawakuweza kujiosha wenyewe kwa sababu hakuna mwenye dhambi anayeweza kuziosha dhambi zake mwenyewe. Musa katika kufanya hivyo alikuwa anahubiri kwa mfano kwamba Yuko Yule awezaye kutuosha dhambi zetu, Mwana wa Adamu Yesu Kristo. Ujumbe huohuo unahubiriwa kila wakati tunapooshwa miguu yetu kabla ya ibada ya ushirika wa meza ya Bwana. Kila mmoja wetu anatenda nafasi ya Kristo tunapooshana mavumbi miguuni kwa mfano wa Haruni na wanawe pamoja na kila kitu katika hema ya kukutania walipotiwa mafuta. Neno upako kwa Kiebrania ni mashiach ambapo neno Masihi linatoka. Kwa hiyo tunaweza kusema walikuwa wamasihi walipopakwa mafuta. Wakawa wawakilishi wa Kristo katika huduma yao. Kwa kuona kwamba sisi sote ni makuhani sasa, swali linakuja: je, u wewe masihi ? Yaani Je, Kristo anaishi maisha Yake ndani yako?

*Mfalme Sulemani alisimama juu ya jukwaa la shaba mbele ya madhabahu na kuwabariki watu. Kisha akapiga magoti na, akiwa ameinua mikono yake juu, akamimina sala ya dhati na kujitoa wakfu kwa MUNGU huku makutano wakiwa wameinamisha nyuso zao chini kwenye ardhi. Baada ya Sulemani kumaliza sala yake, moto wa miujiza ukatoka mbinguni na kuteketeza dhabihu hiyo.

---

Elezea huduma ya asubuhi na mchana kila siku? Ni kabila gani lilichaguliwa kuwa makuhani? Mikate hekaluni ilisimamia nini? Je, unaweza kuelezea mavazi ya Haruni? Mtu aliyekuja na sadaka ya binafsi alifanyaje?

**SIKU YA 43**
**( Februari 12)**

# Utakatifu wa Huduma za Makuhani: Walitengwa ili wamtumikie Mungu, lakini hawakumtumikia kwa muda mrefu

***– Mambo ya Walawi 1- 10***



Makuhani na wote waliotumika kwenye hekalu walikumbushwa na kufundishwa tena na tena kuhusu kazi ya Kristo kwa wokovu wa binadamu. Huduma iliendeshwa kwa makusudi ya kujenga upendo katika mioyo ya watu kwa Mungu na Sheria Yake. Kafara ya kondoo asiye na kosa, ilikuwa ni fundisho la upendo wa Mungu aliyemtuma Mwanawe kuteswa na kufa kwa ajiili ya dhambi zetu. Kamwe tusifikiri Mungu ana hasira nasi, bali tujue kwamba wigo anaotuwekea wa Sheria ni kwa ajili ya usalama wetu. Endapo tutafanya tunalopenda, tutawahuzunisha wenzetu na kisha Mungu pia.

Madhabahu ilikaa katikati ya Waisraeli ikionesha kuwa Mungu Ndiye Mfalme anayetawala katika Israeli, na Walawi wakaweka makambi yao kuzunguka hekalu. Madhabahu ilikuwa Takatifu, ilitengwa au kuwekwa wakfu. Mungu ni Mtakatifu, anataka nasi tuwe wateule na watakatifu kadri inavyowezekana kwa binadamu kuwa mtakatifu. Hebu kijana, na mtoto fikiria katika matendo, nia, maneno au mawazo yako, Je, ni matakatifu? Daudi alisema, "nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele" au "nikae nyumbani mwa Bwana siku zote za maisha yangu, niutazame uzuri wa Bwana" kwenye madhabahu. Madhabahu inaonesha uzuri, haki, na rehema za Mungu. "Njia ya Mungu ipo kwenye utakatifu" Zaburi 77:13. Madhabahu ina mafundisho mazito na makubwa.

Sulemani akizungumza na Mungu alionesha madhabahu kuwa mahali pa kuja kupata msamaha, kupokea kiapo, kuomba kusaidiwa wakishindwa na adui, kuomba Mungu awasaidie wakiwa na ukame, au majanga mengine, kuomba ushindi na hata wageni kuomba.

Baada ya yote yaliyofanyika kuwaweka wakfu watoto wa Haruni kwa kuwavisha mavazi mapya rasmi, mishipi na vilemba haikupita muda, nao waliamua kufanya

uovu. Damu ya kafara ikiwa imewekwa kwenye masikio yao, vidole gumba, na vidole vyao (Mambo ya Walawi 8:24). Mioyo yao bado ilikuwa na mshangao kwa kuona "moto uliotoka mbele za BWANA na kuiteketeza sadaka ya kuteketezwa" ( Law. 9:24 ). Hakika inatupasa kumwomba Mungu uwezo wa kutenda yampendezayo. Kwa hawa vijana, huduma takatifu ya hekalu waliiona ikiendelea siku nzima kila siku na pengine wakaizoea na hivyo hawakujiweka wakfu. Ila kama walisahau waliona paji la uso wa baba yao likiwa limeandikwa "MTAKATIFU KWA BWANA" kwa maandishi makubwa. Walielewa na kujua, kwani baba yao mdogo Musa aliwaeleza vizuri, kwamba walipaswa wawe mfano kwa vijana wengine waliotoka Misri. Walipewa majukumu makubwa, na Mungu alitaka wafuate aliyosema. Walikuwa viongozi wa kiroho kwa vijana wengine wa Israeli. Lakini walikunywa pombe baada ya kuwekwa wakfu. Kwa mtu yeyote awekwaye wakfu, hili ni kosa la kutisha. Damu waliyopakwa masikioni, mikononi na miguuni haikuwasaidia. Hii inatuonesha kuwa pombe iwe mwiko kwetu, maana inapoteza akili na kufanya tusijali vitu vilivyowekwa wakfu, kamwe pombe isiingie mdomoni mwako. Tunaambiwa kuwa "wakatwaa kila mtu chetezo chake, wakatia moto ndani yake, wakatia na uvumba, nao wakatoa moto wa kigeni mbele ya BWANA ambao Yeye hakuagiza. Kisha moto ukatoka hapo mbele za BWANA nao ukawala, nao wakafa mbele za BWANA." Musa akamwambia kaka yake, "Mungu anasema 'Nitatakaswa Mimi katika hao wanikaribiao, Nami nitatukuzwa mbele ya watu hao wote". Haruni alinyamaza kimya. Alipigwa na butwaa na kutetemeka kwa kufiwa na watoto wawili kwa siku moja tena kwa ajili ya kutenda uovu kwa BWANA. Basi Musa akawaita ndugu zao walawi wawachukue nje ya hema, lakini wasilie au kufanya maombolezo yoyote. Mungu alikuwa amewaamini kwa kazi Yake lakini walifanya mzaha. Walifanya vitu vya wakfu kuwa vya kawaida. Hili lilikukwa fundisho kwa vijana, watoto na hata watu wazima pia, wasifanye ujinga huu tena. Walikuwa karibu na Kiti cha Rehema, hivyo dhambi yao ilikuwa kubwa na hata ile rehema haikuweza kuwafunika.

Musa akamwambia baba yao na ndugu zao na jamaa wasiwalilie, na waendelee na ibada. Kisha Mungu akasema, "Msinywe divai wala kileo cho chote, wewe wala wanao pamoja nawe… ili kwamba msife, Amri hii itakuwa ni Amri ya milele katika vizazi vyenu. Kisha mpate kupambanua kati ya yaliyo matakatifu na hayo yaliyo ya siku zote, kati ya yaliyo najisi na hayo yaliyo safi." Hekalu au kanisa la Mungu ni mahali Patakatifu na ibada Yake ni Takatifu. Watu wanapaswa kumcha na kumtukuza.

Hata leo mtoto au msomaji yeyote iwe mwiko kwako kuonja kileo, maana kitakuingiza kwenye dhambi tele. Kuna mafungu zaidi ya 50 kwenye Biblia yahusuyo kutokunywa pombe. Watoto wa Haruni iliwafanya wafanye mzaha na kutojua jinsi ya kutofautisha vitu vitakatatifu, viteule na vile vya kawaida. Wadogo zao Eleazari na Ithamari walishika nafasi zao na wakamfanyia Mungu kazi kwa kicho. Mungu haheshimiwi tunapoingia katika ibada bila kicho. Muziki usio na kicho unapaswa kuepukwa tunapoingia ili kumwabudu Mungu mtakatifu, mambo ya kulakula wakati wa ibada yaepukwe, hata kwa watoto wadogo ni vyema utaratibu uwekwe wa kula na kutofanya muda wa huduma kuwa mrefu na wa kuchosha. Mambo kama kutumia simu wakati wa ibada pia nayo yajaribu kuepukwa kwa

kadri inavyowezekana. Tunapoingia katika siku za mwisho za historia ya dunia, na tumwabudu Mungu kwa uchaji katika roho ya utakatifu na ukweli.

Mistari ya 8-11 yadokeza jinsi pombe waliyoiendekeza ilivyowasukuma Nadabu na Abihu kwenye uamuzi huo wa kizembe. Baada ya tukio hilo, Mungu alizungumza na Haruni akiwaamuru yeye na wanawe wajiepushe na kunywa divai au kileo, ili waweze kuona tofauti kati ya vile vitakatifu na visivyo vitakatifu, na kuwafundisha wana wa Israeli amri za Mungu ipasavyo. Pombe hufunua barakoa ya soni kwenye ubongo wa mtu  na kumfanya afanye yale mambo ambayo  hangeyafanya akiwa na akili zake timamu, kwani angeona aibu au hofu kabisa.

Yesu Kuhani wetu Mkuu, anawakilisha mifano ya huduma ya hema, Yeye sasa Yuko katika Patakatifu pa mbinguni akibeba majina ya watoto Wake wapendwa na kuwaombea watenda dhambi wanaotubu mbele za Baba Yake, tuna uhakika kwamba Yesu hatatusahau kamwe tukimkazia macho anapohudumu katika Patakatifu pa mbinguni. Yabidi tuitoe miili yetu kama dhabihu iliyo hai, takatifu na ya kukubalika mbele za Mungu, kwa njia ya neema ya Kristo, bila ya kuwa na  dosari. Ikiwa hilo laonekana haliwezekani kwetu tudai ahadi hii ya Yuda 1:24 "Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu Wake bila mawaa katika furaha kuu;  Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Kristo Bwana wetu; utukufu una Yeye, na ukuu, na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa, na hata milele. Amina."

*Wahudumu wapige Wagoti kuomba kabla ya Kuhubiri- Kulingana na nuru ambayo tumepewa, ingempendeza MUNGU kwa wahudumu kupiga magoti mara tu wanapoingia kwenye mimbari, na kwa dhati kuomba msaada kutoka kwa MUNGU. Je, hilo lingeleta hisia za ajabu namna gani? Kungekuwa kicho na hofu ya utukufu wa Mungu juu ya watu. Mhudumu wao anawasiliana na MUNGU; anajitoa wakfu kwa MUNGU kabla hajathubutu kusimama mbele ya watu. Kicho kinahisiwa juu ya watu, na malaika wa MUNGU wanaletwa karibu sana. Wahudumu wanapaswa kumtazama MUNGU, mara tu wanapoingia kwenye kibweta, na hivyo kuwaambia wote: MUNGU Ndiye chanzo cha nguvu zangu.

---

Je, Nadabu na Abihu walikufa siku moja kwa sababu gani? Kwa nini kunywa pombe ni dhambi? "MTAKATIFU KWA BWANA" ilionesha nini? Makuhani walimwakilisha  nani  kwenye hekalu? Kwa nini Biblia inasema walevi hawataingia mbinguni? Tumeagizwa mara kwa mara kuweka tofauti kati ya vile vitakatifu na visivyo takatifu, na kati ya vile najisi na safi hii inamaanisha nini? Kuna mahali pengi kwenye Biblia wamesema tusinywe pombe, unaweza kusema mahali pawili?

**SIKU YA 44**
**( Februari 13)**

# Siku ya Upatanisho

**– Mambo ya Walawi 16**



Japo wengi wamepata ugumu katika kusoma kitabu cha Walawi, tujue kwamba kitabu hiki kina mambo mazito yahusuyo wokovu wetu! Wengine katika kusoma Biblia wameita kitabu cha Walawi, na hasa Walawi 16 habari Njema au injili. Huduma za kafara katika Walawi zilikuwa ni kivuli cha kifo cha Yesu msalabani. Hii ilikuwa siku moja ambayo Mungu hakutaka mtu yeyote katika taifa zima la Israeli asahau. Mtazamo uligeuka kutoka kwa damu iliyomwagika hadi damu iliyowekwa au kupakwa ili kuonyesha mfano wa wokovu wetu unavyokuja kupitia damu ya Masihi. Wakati huduma za kila siku zilipokuwa zikiendelea, mara moja kwa mwaka kulikuwa na ibada inayojulikana kwa Wayahudi kama Yom Kippur, yaani Siku ya Upatanisho. Kila mtu alipaswa kuonyesha uadilifu kwa Mungu kwa kujikana nafsi. Ikiwa walikuwa wazembe au wasiojali kuhusu kile kilichokuwa kikiendelea ndani ya pazia, walipata adhabu ya kifo. Mbuzi wawili walichaguliwa, lakini ni mmoja tu, ndiye aliyetolewa dhabihu. Huyu aliitwa mbuzi kwa ajili ya Bwana. Damu yake ilinyunyizwa juu ya kiti cha rehema, kwa njia ya mfano kutakasa Patakatifu kwa dhambi zote ambazo zilisamehewa katika mwaka huo. Yule mbuzi mwingine alitumwa akiwa hai kutoka Patakatifu hadi nyikani, yaani nchi isiyokaliwa na watu, na kuachwa peke yake ili afe. Hii ilikuwa siku kuu, na pia ilikuwa siku ya furaha kubwa. Kwa wale ambao walikuwa wakizingatia umuhimu wake na hawakuiondoa akilini mwao, ilikuwa siku ya utakaso na ushindi. Na hili linaweza kuwa kwetu leo! Maandalizi yamefanywa kwa ajili ya utakaso na ipo siku inakuja ambapo dhambi haitakuwapo tena!

Siku hii kuu katika taifa la Israeli, yaani siku ya upatanisho (Yom Kippur/ Atonement), watu wote waliacha kazi zao. Kabla ya siku hii watu waliambiwa wajitayarishe kwa kujihoji dhambi zao, na kujutia dhambi walizozifanya. Ni kuhani mkuu tu ndiye ambaye aliruhusiwa kuingia Patakatifu pa Patakatifu. Na hata

yeye angeingia huko mara moja tu kwa mwaka, siku iliyoitwa "siku ya upatanisho." Ikiwa angekiuka hili angeuawa mara moja. Huduma ya siku hiyo ya upatanisho ilifanya watu wajue kuwa 'kila binadamu amefanya dhambi na kupungukiwa utukufu wa Mungu,' na wanapaswa kumwomba Mungu azioshe dhambi zao. Kila mtu alipaswa kufunga siku hiyo, mpaka wakati huduma ya upatanisho ilipokuwa imemalizika. Watu walipaswa kuonesha huzuni na majuto kwa dhambi zao, na kumkaribia Mungu kuomba msamaha na rehema. Watu walipaswa pia kuwa na usafi wa mwili ili kukutana na Mungu wao. Hata leo ni vyema tuoge na kuondoa taka za mwili, na kisha kufua nguo zetu ili ule uchafu wake usifyonzwe na kurudi tena kwenye miili yetu na kisha ukarudi kwenye ngozi na damu tena.

Asubuhi ya siku hiyo, kuhani mkuu alitoa dhabihu ya ng'ombe dume na kuteketeza kwa dhambi zake mwenyewe na familia yake. Alichukua damu ya huyu ngombe na kupita nayo mpaka Patakatifu na kisha patakatifu pa patakatifu na kuinyunyiza kwenye mfuniko wa dhahabu wa sanduku la agano. Hii ilionesha naye pia ni mkosaji, anayeomba rehema, msamaha na toba toka kwa Mungu. Kuhani alipaswa kuombea dhambi zake zisamehewe kwanza kabla ya kuombea wengine.

Kisha kuhani angekuja mbele ya madhabahu ya kuteketeza kafara na mbuzi wawili wangeletwa kwake. Hawa mbuzi wawili waliwakilisha kubeba dhambi za watu. Yule wa "kwa Bwana" alichinjwa na kuteketezwa kwenye madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa pale hemani. Kuhani alichukua damu na kuingia Patakatifu pa Patakatifu na kunyunyuzia damu kwenye sanduku la agano akimwomba Mungu apokee sadaka hiyo na kusamehe dhambi za wana wa Israeli. Kuhani alikuja nje tena na kuweka mikono yake juu ya yule mbuzi wa azazeli, ikimaanisha mfano wa kuweka dhambi za watu juu ya yule mbuzi. Mbuzi huyu aliitwa 'mbuzi wa azazeli' na alichukuliwa nyikani, mbali sana ambapo asingeweza kujua njia ya kurudi tena na huko akaachiwa huru. Hii ilionesha kuwa "dhambi za watu zimechukuliwa na kutengwa mbali nao.

Huduma hii ilipoisha, watu waliamini kwamba Bwana amewasamehe dhambi zao na kuzisahau. Kisha dhabihu za kawaida za mchana ziliendelea kwenye madhabahu ya sadaka ya kuteketeza, na watu wangeenda nyumbani kwa furaha, na kufungua mfungo wao wa toka jana yake.

Mungu aliweka haya ili watu wajue kwamba dhambi ni jambo zito na la huzuni, kwani inatutenganisha na Mungu na kuleta kifo. Dhambi yaweza kuondolewa tu, kwa njia ya damu ya Yesu. Kama Mungu Mwenye uwezo wote hakuweza kupata njia nyingine ya mkato ila Mwana Wake Afe, basi, dhambi ni kitu kizito, tusichukulie kirahisi tukikenua meno. Damu ya wanyama ilikuwa mfano tu, wa Yesu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Kabla Yesu hajaja, Mungu aliwaonesha njia ya msamaha na amani.

Kile kuhani mkuu alichofanya siku ya upatanisho ndicho Yesu alianza kufanya katika Patakatifu pa mbinguni Oktoba 22, 1844 kutokana na unabii wa Daniel 8 na 9. Akiwa katika Patakatifu pa Patakatifu akipatakasa Patakatifu pa mbinguni kwa njia ya hukumu ya upelelezi, hivi leo dhambi bado zaweza kuungamwa na

kusamehewa. Lakini Anapomaliza mchakato huo, siku moja hivi karibuni, rehema inafungwa kwa wanadamu. Hapo ndipo Atakapotangaza: "Mwenye kudhulumu na aendelee kudhulumu; aliye mchafu na aendelee kuwa mchafu; mwenye haki na azidi kufanya haki; aliye mtakatifu na azidi kutakaswa." Ufunuo 22:11

Ikiwa kulikuwa na wakati wowote ambao Wakristo tunapaswa kuwa na kiasi, na kutesa nafsi zetu kwa kufunga na kuomba-kukiri na kuacha dhambi zetu, ili wakati rehema itakapofungwa siku moja hivi karibuni, tutakuwa tumetiwa muhuri milele kama watoto wa Mungu ni sasa hivi. Kivuli cha haya yote ya kafara kilielekeza dhabihu ya mara moja tu ya Yesu Kristo Mwenyewe.

Ninashukuru kwamba Yesu anatusafisha kwelikweli na dhambi zote. Ni lazima tuungame dhambi zetu katika sala kwa Yeye ambaye ni "mwaminifu na wa kweli hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote"! 1 Yohana 1:9. Amina! Huo ndio utumishi uliofanywa "kwa mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni." Na kile kilichofanywa kwa mfano katika huduma ya Patakatifu pa kidunia kinafanywa kwa uhalisi katika huduma ya Patakatifu pa mbinguni sasa. Baada ya kupaa Kwake Mwokozi wetu alianza kazi Yake kama Kuhani wetu Mkuu, akituombea na kutupatanisha na Baba wa mbinguni. Paulo asema hivi: "Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanywa kwa mikono, palipo mfano wa Patakatifu halisi, bali aliingia mbinguni kwenyewe, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu. Waebrania 9:24.

Haruni alilazimika kutumia saa nyingi kujitayarisha kukutana na Mungu, lakini sisi tunaweza kumkaribia Mungu hivi leo wakati wowote (Waebrania 4:16). Ni upendeleo ulioje kwamba tumepewa kumfikia Mungu kirahisi kuliko makuhani wakuu wa nyakati za Agano la Kale, lakini hatupaswi kamwe kusahau utakatifu wa Mungu na kumkaribia Yeye bila kicho. Yesu ametupa njia rahisi ya kumkaribia Baba Yake kwa hiyo hebu tuiandae mioyo yetu kabla ya kuja mbele Zake kwa maombi.

*Sababu kwa nini wengi wameachwa peke yao katika maeneo ya majaribu ni kwamba hawakumweka Bwana mbele yao daima. Tunaporuhusu ushirika wetu na MUNGU uvunjwe, ulinzi wetu unatoweka kwetu. Sio madhumuni yako yote mazuri na nia njema ndiyo vitakuwezesha kuhimili uovu. Lazima muwe wanaume na wanawake wa maombi. Maombi yenu hayapaswi kuzimia, kuwa ya msimu hapa na pale unapoamua, na ya kuzimiana kuamka kama kifafa, bali ya bidii, ya kudumu, na ya daima. Si lazima kila wakati kupiga magoti ili kuomba.

---

Siku ya upatanisho ilifanyika mara ngapi kwa mwaka? Kwa nini watu walifunga? Kwa nini kuhani alianza kuomba msamaha kwake kwanza? Je, mbuzi wawili waliwakilisha nini? Kwa nini watu walienda nyumbani kwa furaha? Je, yule mbuzi aliyepelekwa nyikani anamwakilisha nani? Je, kwa nini hakuna haja ya kutoa kafara siku hizi? Hekalu lilijengwa kutokana na mfano wa nini kule mbinguni? Walawi 16 na Isaya 53 zinazungumza kuhusu nini? Kazi ya ukuhani ilihusu vipengele vingi na hatua kwa hatua, unafikiri waliwezaje kuifanya kazi hii kwa ubora au uadilifu? Unaweza kuelezea changamoto ambazo ungekuwa nazo kama ungetoa kafara ya kuchinja kondoo kila unapotenda dhambi leo.

**SIKU YA 45**
**( Februari 14)**

# Najisi na Visivyo Najisi

**- Walawi 11-19**



Mungu akawaambia wana wa Israeli aina ya vitu vilivyo halali kuliwa na visivyo halali. Waliambiwa wale wanyama wenye kwato katika miguu na wale wanaocheua kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, swala, n.k. Bali nguruwe, ngamia, simba au tembo waliambiwa wasile kwa vile wana moja kati ya sifa mbili za mnyama anayefaa kwa kuliwa, mnyama anayepaswa kuliwa anahitajika awe na kwato zilizopasuliwa zikawa mbili na tena awe anacheua. Nguruwe hacheui japo ana kwato, na sungura anacheua lakini hana kwato. Kisha upande wa samaki waliambiwa wa kuliwa ni wenye mapezi na magamba tu. Hivyo pweza, na kamba na wengineo wasio na sifa husika ni najisi. Kisha kuhusu ndege, waliambiwa kuwa wasile wale ambao wanakula mizoga, kama vile tai, kunguru, dudumizi, bundi, mnandi, n.k. Waliruhusiwa kula kuku, kanga, njiwa, n.k. Kwa vile vitambaavyo vyenye mabawa, waliruhusiwa kula wale walio na miguu mirefu ya kurukia juu ya nchi kama vile panzi, nzige na parare, bali wasile kumbikumbi. Leo wataalamu wamegundua kuwa nguruwe ana minyoo kwenye minofu yake naye hula cho chote, na kuletea watu magonjwa, wengine bila kujali hula nyama hizi na hivyo wanahatarisha afya zao, na hali Mungu alishawaonya mapema. Mungu Ndiye anayejua kile kinachofaa miili yetu. Maelekezo hayo ni kwa faida ya miili yetu na afya zetu kiroho na kimwili. Kuendekeza ulaji wa nyama, hudhoofisha nguvu za kimwili, kiakili, na kimaadili. Bwana atawapa watu Wake hekima ya kutayarisha chakula kutokana na mazao ambayo ardhi au hali ya hewa hutoa, na vyakula vitakavyochukua mahali pa nyama. Kwani kabla ya maduka watu walikuwa na mifugo ambayo wasingechinja kila siku. Nao walikula nyama mara chache chache, ila leo tuna maduka na hivyo

wale wenye uwezo wanaweza kufanya makosa ya kula nyama au samaki kila siku, na hilo likiendekezwa au lisipofanyiwa mpango vizuri laweza kuleta magonjwa ya moyo, kolestroli, kansa na mengineyo kwao kiurahisi, kuliko ambavyo wala vyakula vya mimea wanavyosumbuliwa.

Unapotafakari juu ya chakula unachoweka kwenye meza yako kila siku, fanya vile ajili ya "utukufu wa Mungu." (1 Wakorintho 10:31 ) Mungu anataka tuwe na afya njema, furaha, na utakatifu katika kila nyanja ya maisha yetu. Hii ndiyo sababu ametupa mipaka katika vile tunavyopaswa kuweka mdomoni tokea bustani ya Edeni maana inaathiri mionjo ya kiroho na kimaadili pia wakati mwingine. Hatupaswi kuendekeza uchu wa chakula au kuwa na ulafi. Ulaji wetu wapaswa uwe na busara na kiasi. Ikiwa mazoea ya kula na kunywa yanawekwa chini ya udhibiti wa mwanadamu, naye anakula na kunywa kwa utukufu wa Mungu, maisha yake yataongezwa. Tunapaswa kula ili tuishi na si tuishi ili tule. Tusifanye matumbo kuwa miungu yetu; viungo vyetu vya usagaji chakula vitachoshwa na mashine zake zitapelekea kupata magonjwa mabaya, na furaha yetu itaharibiwa na hayo mazoea yao mabaya.

ingawa tunapenda nyama, Mungu aliyeumba viumbe hawa anajua kilicho bora kwetu. Magonjwa mengi ya kutatanisha leo ni matokeo ya lishe duni. Hebu turejee Edeni na tufurahie maisha yenye afya hadi Yesu atakapokuja. Tunahitaji afya zetu zitusaidie kukabiliana na kile kinachoijia dunia hivi karibuni. Gharika ndiyo ilipelekea kula nyama, ila leo hakuna gharika, na hivyo tunashauriwa kurudi kwenye lishe yetu ya mimea. Imethibitishwa kisayansi kuwa lishe inayotokana na mimea inakuza afya njema na kusaidia kuzuia kutokuwepo magonjwa ya kuambukiza.

Mungu akawapa sheria pia za afya. Sheria hizi zilikuwa za kusaidia watu wengi kama hawa jangwani wasipate magonjwa na kuambukizana. Waliambiwa kufua mavazi yao, kufunika choo kwa jembe wakijisaidia. Walipaswa kuwa safi, maana Mungu ni Mtakatifu, akawaambia wawe wasafi, isije kuwa anakuja kuwabariki, ila kwa uchafu wao au unajisi akaghairi.

Wakapewa sheria za kutoka damu, au mafuta, hii yawezekana ni kwa ajili ya magonjwa pia. Hata wale wenye nyumba zenye Kuvu (fangasi) walipewa maagizo jinsi ya kuondoa fangasi na ikishindikana wachome nyumba hizi moto. Siku hizi watu wengi wamegundua kwamba fangasi kwenye nyumba ni jambo la hatari na limeua wengi, waliovuta hewa yenye fangasi. Wale wenye magonjwa yanayotoa usaha au maji maji mwilini walipaswa watengwe kwa muda watokane na hali hii ili wengine wasipate maambukizo. Mungu akaendelea kuwapa Sheria za kuishi pamoja mfano, wasivune kila kitu bali wasaze ili maskini au mgeni au mtu baki aokote. "usimlaani kiziwi wala usitie kwazo mbele ya kipofu, bali umche Mungu wako. Mimi Ndimi Bwana. Msitende yasiyo haki katika hukumu." Wakaambiwa wasiwe wachongezi, wasichukie watu mioyoni mwao au kuweka kisasi wala kuwa na kinyongo au kukaa na mwanamke au mume bila ndoa. Wakaambiwa pia wasioane au kulala na jamaa wa karibu, wasichukue mke au mume wa ndugu au kulala na mnyama au mwanamume kwa mwanamume au mwanamke kwa mwanamke. Watu wakisoma hushangaa kwamba maovu yalianza zamani tu. Hebu tugundue kwamba

Shetani ni yule yule, na anatesa watu mpaka atakapoangamizwa.

Maagizo yakatolewa "msiwaendee wenye pepo, wala wachawi ... Mimi Ndimi BWANA Mungu wenu." Wakaamriwa waondoe wachawi au wote wanaojihusisha na nguvu za giza. "Mwondokeeni mwenye mvi; heshimuni uso wa mtu mzee". Wakaambiwa wamjali na kumpenda mgeni, yatima na mjane, na kuwasaidia kama nafsi zao bila ya kuwadhulumu. Hili ni muhimu kwetu leo kama watoto. Tusifanye ubaguzi wa mtoto mgeni akija shuleni, au jirani mpya aliyehamia karibu nasi. Watu wengi katika Biblia walikuwa wahamiaji, na wageni na wakawa mbaraka kwa kukaribishwa na wengine. Waweza kutaja majina ya wahamiaji kwenye Biblia? Nchi zetu pia zina wakimbizi, twapaswa kuwa watu wenye fadhila.

Walawi wafanyao kazi madhabahuni waliagizwa la kufanya wakihudhuria mazishi na kuwa najisi, wakaagizwa pia waoe mwanamke ambaye hakuolewa na mtu mwingine au asiyetanga tanga huku na kule. Wakapewa maagizo ya kutojichanja chale mwilini. Siku hizi watu wengi wa magharibi wanajichanja chale za kutisha kwa kupenda kwao, japo wengi zamani Afrika walilazimishwa na wanajaribu kuzifuta. Soma zaidi haya kwenye Walawi kitabu chote, na ile sura ya 19 pia. Kuhani alipaswa awe mkamilifu kwa tabia na hata kwa maumbile pia asiwe na kilema akimwakilisha Mungu.

Wakaambiwa wasile nyamafu, yaani mnyama asiyechinjwa, kwa usalama wao wa afya na kujiweka wakfu. Walipaswa kutoa mnyama aliye kamili kwa kafara, pia asiye na kilema cho chote.

Mtu yeyote ambaye analiapiza Jina la BWANA na kukufuru angeliuawa. Walipaswa kusaidia ndugu zao, na waingiapo Kanaani kuilima ardhi miaka sita na kuiacha nchi mwaka wa saba kwa ajili ya maskini kuokoteza chakula. Wakakatazwa kutengeneza sanamu na kuziabudu. Leo hatutengenezi sanamu ila fikiria kitu unachokipenda zaidi ya Mungu, hiyo ni sanamu, yaweza kuwa chakula, nguo, vitu vya kuchezea, kompyuta, televisheni au mtu.

Mungu akatoa Sheria za kuweka nadhiri na umuhimu wa kuzitunza. Hata leo unaweza kutoa nadhiri Mungu akikusaidia jambo utatoa sadaka au kufanya jambo Fulani la kushukuru. Kumbuka kutunza nadhiri hii, unapoiweka, ili usifanye mzaha na Mungu.

Maelekezo haya mengi ambayo ni kama taa za barabarani (trafiki laiti), hakika yanahusiana na wajibu wa watu kwa Mungu, wao kwa wao, na kwa watu baki. Twaweza kusema hizi ni Amri Kumi zilizochambuliwa zaidi na kutolewa kwa namna maalum, na mtu akizielewa hana haja ya kukosea. Hizi zilikusudiwa kulinda utakatifu wa amri kumi ambazo zilizochongwa kwenye mbao za mawe. Yesu akamwambia Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri kuu na ya kwanza. Na ya pili inafanana nayo, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii. Mathayo 22:38-40. Ni kawaida sana kwa wanadamu kulipiza kisasi wanapokosewa, lakini hapa tunaambiwa tusilipize kisasi. Kinachotupa uchungu

tunapoambiwa tusilipize kisasi ni kuwaza kuwa mkosaji ataachiwa huru. Lakini hilo siyo, kwani atavuna alichopanda, kwa maana Biblia inasema: "Wapenzi, msijilipizie kisasi, bali ipisheni ghadhabu; kwa maana imeandikwa, Kisasi ni Changu Mimi, Mimi nitalipa, asema Bwana. Kwa hiyo "Adui yako akiwa na njaa, mpe chakula; akiwa na kiu, mpe maji ya kunywa; Maana kwa kufanya hivyo utampalia makaa ya moto juu ya kichwa chake." Warumi 12:19-20

Mungu anatawala, Naye ni Mungu wa haki na mkamilifu. Hebu tumpe kesi zetu na badala ya kuwa na kinyongo dhidi ya wale wanaotuumiza, tuombe neema ya kuwapenda bila masharti. Kwa kufanya hivyo, tunaakisi tabia ya Baba yetu wa mbinguni ambaye "huangazia jua Lake juu ya waovu na wema, na kuwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki." Mathayo 5:45 . Lakini "kwa vyovyote si kuwaondolea hatia. . ." Kutoka 34:7

Utakatifu si wa kunyakuliwa kwa nguvu: bali ni kuyasalimisha mapenzi yote kwa Mungu; ni kuishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu; ni kufanya mapenzi ya Baba yetu wa mbinguni; ni kumtumaini Mungu katika majaribu, giza na nuru; ni kutembea kwa imani na si kwa kuona na macho yetu; ni kumtegemea Mwenyezi Mungu kwa ujasiri usio na shaka, na kutulia katika upendo Wake. Mioyo yetu ni miovu, na hatuwezi kuibadilisha.... Elimu, utamaduni, utekelezaji wa nia, au juhudi za kibinadamu, vyote vina nyanja yake sahihi, lakini havina nguvu. Vinaweza kuzalisha usahihi wa nje wa tabia, lakini haviwezi kuubadilisha moyo; haviwezi kuitakasa chemchemi za uzima. Neema yake pekee ndiyo inayoweza kuhuisha uwezo usio na uhai wa nafsi, na kuivuta kwa Mungu, kwenye utakatifu.

Utakatifu ni zawadi ya Mungu kupitia Kristo. Wale wanaompokea Mwokozi wanakuwa wana wa Mungu. Wao ni watoto Wake wa kiroho, waliozaliwa mara ya pili, waliofanywa upya katika haki na utakatifu wa kweli. Akili zao zimebadilika. Wanaona uhalisi wa milele kwa maono yaliyo wazi zaidi. Wanafanywa wana katika familia ya Mungu, na wanafanywa kufanana na sura Yake, wakibadilishwa na Roho Wake kutoka utukufu hadi utukufu. Wanakuja kuthamini upendo mkuu kwa Mungu na Kristo.... Wanamkubali Kristo kama Mwokozi wao binafsi, na kufuata mfano Wake wa kujikana nafsi—hii ndiyo siri ya utakatifu. BWANA akamaliza kwa kuwakumbushia kwamba mzaliwa kwa kwanza wa mnyama au mtu ni Wake,

*Kuza tabia ya kuzungumza na Mwokozi unapokuwa peke yako, unapotembea, na unapokuwa na shughuli nyingi zinazohusiana na kazi zako ya kila siku. Acha moyo uinuliwe kila wakati katika ombi la kimya la msaada, kwa ajili nuru, nguvu, ufahamu na maarifa. Hebu kila pumzi na iwe sala.

*Katika kazi ya kutunza mioyo ni lazima tuwe na utayari katika sala, bila kuchoka katika kukiomba kiti cha neema kwa ajili ya msaada. Wale ambao huchukua jina la "Mkristo" wanapaswa kumjia MUNGU kwa dhati na unyenyekevu, wakisihi msaada. Mwokozi ametuambia tuombe bila kukoma. Mkristo hawezi kuwa katika mkao wa kuomba kila wakati, lakini mawazo na matamanio yake yanaweza kupanda kuelekea juu kila wakati. Kujiamini nafsi zetu wenyewe kungetoweka, kama tungeongea kidogo na kuomba zaidi.

Kwa nini nguruwe na pweza ni najisi kula? Je, kwa nini ni muhimu kutunza nadhiri zetu kwa Mungu? Je, kwa nini wasingelima mwaka wa saba wakiwa Kanaani? Kwa nini tunaamriwa tusiwaendee wachawi? Kwa nini ni dhambi kumbagua mtu wa kabila jingine au mgeni? Kwa nini hatupaswi kuchanjwa chale? Wengine wamechanja miili kabla ya kusoma Maandiko kwamba tusichanje miili, je, tukiwalaumu watu hawa tutakuwa tumetenda haki? (tattoo)

**SIKU YA 46**
**( Februari 15)**

# Mungu na Watu Wake Wanaolalamika

**- *Mambo ya Walawi 26, Hesabu 1 na 7 na 11***

Kitabu cha Hesabu kinapoanza watu wanahesabiwa na kutoa matoleo maalumu kutokana na makabila yao 12 na viongozi wa makabila ndiyo wanaotoa. Ukarimu ni jambo la muhimu sana. Jaribu kulinganisha sensa hii na ile ya kutoka Misri. Walawi walikuwa fungu la BWANA kama vile mzaliwa wa kwanza alivyokuwa wa BWANA. Nasi leo ni vyema kuweka watoto wetu wakfu kwa BWANA. Tuna Mungu wa ajabu sana, Mwenye neema kama nini! Anatafuta kutuokoa kwa kila njia iwezekanavyo. Anatupa baraka za kila aina, na angefurahi kutupa zaidi ikiwa tungeweza kustahimili baraka hizo. Ikiwa tutaanguka katika dhambi na kumkataa, lakini baadaye tutubu, atatukubali tena kwa neema na kurejesha baraka Zake. Nashukuru uadilifu wa mchakato wa kuhesabu watu. Mwakilishi wa kila kabila alikuwepo wakati wa sensa. Hii ilihakikisha haki na uhalali wa matokeosahihi. Mungu ni Mungu wa utaratibu na mipango. Ni lazima tujitahidi kwa uadilifu na juhudi zetu zote kuenenda katika maagizo Yake. Na kisha Bwana wetu Yesu anatuonya kwamba “Walioitwa ni wengi, lakini waliochaguliwa ni wachache.” Mathayo 22:14. Ni wale tu wanaosalimisha maisha yao kikamilifu kwa Mungu na bila ya kujibakiza ndio watakaofika mbinguni. Hebu tuazimie kuwa miongoni mwao.

Haukupita muda baada ya Nadabu na Abihu kufa, watu wakaona wingu linakaa na linasogea kwenda nchi ya ahadi. Wakasafiri siku tatu, na likasimama na Walawi wakaweka madhabahu na makabila 12 yakapiga kambi kuizunguka. Watu wakafurahi kwamba angalau wanasogea kwenda nchi ya ahadi. Kwa kweli hawakuwa tayari na mafundisho mengi ambayo Mungu alikuwa anataka wayapate. Waliona miujiza ya bahari ya Shamu, Mana, na mengineyo, lakini imani yao bado ilikuwa dhaifu. Muda si mrefu, watu wakaanza kunung’unika, kuhusu jangwa na kusema afadhali wangerudi Sinai.

Hata leo tuepuke manung’uniko, maana BABA yetu wa mbinguni anatupenda na kutupatia mahitaji yetu. Tumwambie shida zetu na kuwa na imani kuwa atatenda. Mungu hajibu malalamiko, bali anajibu maombi. Basi Wengine wakataka chakula cha mifugo au maji. “BWANA aliposikia hayo, hasira Zake zikawaka na moto wa BWANA ukawaka kati yao, ukateketeza katika mipaka ya mwisho ya marago.”Watu wakamlilia Musa, naye akawaombea na huo moto ukakoma, mahali hapa pakaitwa Tabera, kwa sababu huo moto wa BWANA ukawaka kati yao. Manung’uniko hayakuishia hapo kwani watu waliochanganyika nao walianza kulalamika tena na Waisraeli wakajiunga nao. Shida ilikuwa ni chakula, walisema, wamechoka kula mana. Wakalilia nyama walizokula bure huko Misri, na matango, matikitiki, mboga na vitunguu na hata vitunguu saumu, walisema, “lakini sasa roho zetu zimekauka; hapana kitu cho chote; hatuna cha kutumaini isipokuwa hii mana tu. Kwa kweli mana iliweza kuandaliwa kwa aina tofauti, kuisaga, kuioka, kuichemsha, n.k. Hata



leo tuna ulafi na hamu ya vyakula au vileo visivyofaa, na tunapuuzia chakula Mungu alichotupatia, na kulalamika, badala ya kula kwa shukurani. BABA yetu, tungemwendea na kumwambia tunavyojisikia, lakini kwa heshima. "BABA hii mana leo imenishinda kula, Je, una kitu kingine utusaidie tubadilishe chakul au lishe leo. Kweli Mungu atupendaye angekataa kweli? Mbona wengi wa baba zetu wa dunia wanatufanyia mengi?

Musa alisikia watu wakilia. Hasira ya Bwana ikawaka sana na Musa naye akakasirika akasema "BWANA mbona umenitenda uovu mimi mtumishi wako? Kwa nini sikupata neema machoni pako, hata ukanitwika mzigo wa watu hawa wote juu yangu?… Je, Mimi Ndiye nimewazaa hawa wote hata wewe kuniambia, Haya, wachukue kifuani mwako, mfano wa baba mwenye kulea achukuavyo mtoto anyonyaye au uende nao mpaka nchi uliyowaapia baba zao? Nipate wapi nyama ya kuwapa watu hawa wote? Kwani wananililia tupe nyama tupate kula. Mimi siwezi kuwachukua hawa wote peke yangu, kwa kuwa ni mzigo mzito sana wa kunishinda. Na kama ukinitenda hivi, nakuomba uniulie mbali, kwamba nimepata fadhili mbele ya macho yako; nami nisiyaone haya mashaka yangu" tena.  Kweli Nabii Musa alilemewa mpaka akatamani Mungu ampumzishe.

Mungu alikuwa ameshawafanyia mengi, na kuwaahidi mengi si mvua, si amani "na watu watano wa kwenu watafukuza watu mia, na watu mia wa kwenu watafukuza watu elfu kumi, na adui zenu wataanguka mbele yenu kwa upanga… nanyi mtakula akiba ya zamani mliyoiweka…Nami nitaweka maskani yangu kati yenu; wala roho

yangu haitawachukia. Nami nitakwenda kati yenu, Nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu Wangu, Mimi Ndimi BWANA Mungu wenu, niliyewaleta mtoke katika nchi ya Misri" ya utumwa na kongwa.

Akasema wakizikataa Amri, ataleta utisho…." Mtapanda mbegu yenu bure, kwa kuwa adui zenu wataila… mtapigwa mbele ya adui zenu… watawatawala na mtakimbia wakati ambapo hapana awafukuzaye…Nami nitavunja kiburi cha uwezo wenu…nitawapiga …mara saba kwa ajili ya dhambi zenu…mtakula nanyi hamtashiba". Mausia haya yalikuwa mazito, Mungu ni upendo ila Maagizo na Amri Zake tunapaswa kuzifuata, kwa faida yetu wenyewe na hata wenzetu. Je, umeshawahi kufikiri kwamba itakuwaje kama kila mtu atafanya anachotaka tu, na asifuatae Sheria? Jaribu kuchukua dakika tano kutafakari. Mungu ni Mwenye rehema ila tunapokuwa waasi wakati wote, na kutotaka awe kiongozi wetu, basi hukumu Zake ni lazima zifanyike, tusisahau hili.

BWANA akamwambia Musa achukue wazee 70 wa Israeli naye atawapa roho ya Musa ndani yao, nao watamsaidia kuchukua mzigo wa watu pamoja nawe, ili usiuchukue wewe peke yako. Akaambiwa awaambie watu wajitakase nafsi zao na kabla ya kesho watakula nyama, kwa maana walilia nyama na kusema kule Misri walikuwa na uheri. BWANA akasema hawatakula kwa siku chache bali mwaka mzima mpaka itakapotoka katika mianzi ya pua zenu nanyi mtaikinai". Kwa sababu walimkata BWANA aliyewatoa Misri na kulia "tulitoka kwa maana gani?". Musa akashangaa watu wote watapataje nyama, hata makundi ya kondoo au ng'ombe yakichinjwa au samaki wote wa baharini wakikusanywa kwa watu hawa mamilioni itatosha kweli. BWANA akamwambia Musa "Je! Mkono wa Bwana umepungua urefu Wake?" Musa akawafahamisha haya wazee 70 na watu wote. Bado kazi ilimlemea japo alifuata mashauri ya Yethro. Basi watu 70 walipewa roho ya Musa na kuanza kutabiri, ila Eldadi na Medadi ambao ni kati ya wale 70 walikuwa wapo kambini na si kwenye mkutano. Yoshua aliposikia alimsihi Musa awakataze bali Musa akajibu, "umekuwa na wivu kwa ajili yangu; ingekuwa heri kama watu wote wa BWANA wangekuwa manabii na kama Bwana angewatia Roho Wake". Musa hakuona wivu, Mungu akitumia watu wengine kumfanyia kazi, nasi tusiwaonee wivu watu wengine.

Bwana akaleta kware wengi mno, na kila mtu akala mpaka akasaza. Kware ni wagumu kuwashika, ila hawa waliletwa na BWANA! Nyama ilipokuwa ingali kwenye meno bado wakitafuna na zingine wamezibanika kuzunguka kambi. Ndipo hasira ya BWANA ikawaka, na wakapigwa na pigo kuu kwa manunguniko na ulafi au tamaa. Wakapaita pale Kibroth-Hataava maana yake walipozika hao watu waliotamani. Mungu anataka tuwe na afya njema, furaha, na utakatifu. Hii ndiyo sababu anataka tule vile alivyoagiza, na kisha tuache yale ambayo si bora kwa afya zetu. Watu wanaoishi vibaya, kwa kuendekeza ulaji wa chakula kingi, wanateseka kutokana na kuendekeza uchu wa kula. Matengenezo ya tabia zao katika kula na kunywa yanahitajika. Lakini mageuzi haya hayawezi kufanywa mara moja. Mabadiliko hayo lazima yafanywe hatua kwa hatua. Vyakula vya afya vinavyowekwa mbele yao lazima viwe vya kupendeza na kuleta hamu ya kula. Maisha yao yote, pengine, wamekula milo mitatu kwa siku na wamekula chakula kingi sana. Ni jambo muhimu wafundishwe jinsi ya kula kwa afya na kuwa na kiasi.

Chakula wanachopewa, lazima kiwe imeandaliwa vyema, na lazima na lishe nzuri zaidi.

*Njia ya kwenda kwenye kiti cha enzi cha MUNGU iko wazi kila wakati. Hutaweza kupiga magoti kila wakati kwa ajili ya maombi, lakini maombi yako ya kimya yanaweza kupaa juu kwa MUNGU kila wakati kwa ajili ya nguvu na mwongozo. Utakapojaribiwa, kama itakavyokuwa, unaweza kukimbilia mahali pa siri Pake Yeye Aliye Juu. Mikono Yake ya milele itakuwa chini yako. Acha maneno haya yakutie nguvu, “Lakini wako wachache huko Sardi ambao hawakuyachafua mavazi yao; nao watakwenda pamoja nami wakiwa wamevaa mavazi meupe, kwa maana wamestahili.” Ufunuo 3:4.

---

Kwa nini manung’uniko ni dhambi? Moto ulitokeaje? Orodhesha manung’uniko au malalamiko uliyo nayo, na kuona yapi ni dhambi? Wazee 70 walihusika na nini? Kwa nini Yoshua aliona wivu? Kware walitoka wapi? Kwa nini ulafi ni dhambi?

**SIKU YA** 47
**( Februari 16)**

# Ndugu wa Musa na Uasi

**- Hesabu 12 na 16**

Haikuchukua muda Miriamu, dada yake Musa, na kaka yake Haruni wakaanza kumsengenya Musa, na kumwonea wivu. Mara nyingi mtu wa karibu akitufanyia hiana, tunapata uchungu zaidi ya 'mpita njia.' Miriamu alikuwa dada mzuri ambaye ndiye aliyemwita binti Farao ili Musa akae na mama yake akitunzwa, alikuwa amefanya kazi na kaka yake toka Misri na kuwaleta watu mpaka hapo walipofikia. Ila sasa Miriamu akaanza kuonesha ubaguzi "wakimnenea Musa kwa sababu ya mwanamke mkushi aliyekuwa amemwoa." Tafsiri zingine zinasema kwa sababu alikuwa mweusi, hapa kwetu Afrika tutasema kwa sababu alikuwa wa kabila jingine. Shida hii inatokea kwa mawifi au wakwe wengine hata siku hizi, tujihadhari na uovu wa kutesa ndugu na dada eti kwa sababu wametoka kabila jingine. Kinachotakiwa tu ni awe mtu wa imani, na hata hivyo baba yake Sipora alikuwa kuhani wa Mungu wa Ibrahimu, naye pia alikuwa anamhimidi Mungu wa Kweli.

Mungu akaingilia kati, akawaambia, "akiwapo nabii kati yenu, Mimi Bwana nitajifunua kwake katika maono, Nitasema naye katika ndoto … Ila mtumishi Wangu Musa … ni mwaminifu … kwake nitanena mdomo kwa mdomo … wala si kwa mafumbo, na umbo la Bwana yeye ataliona. Mbona basi ninyi hamkuogopa kumnenea mtumishi Wangu huyo Musa?" Basi Miriamu akapata adhabu ya ukoma mweupe kama theluji. Haruni akamsihi Musa amwombe Mungu ili dada yao apone "tumefanya upumbavu na kufanya dhambi. Nakusihi." Musa akamwomba Mungu. Miriamu akawa na ukoma siku saba akikaa nje ya kambi, wala watu hawakusafiri mpaka Miriamu alipoletwa tena . Dhambi ya mtu mmoja ikawachelewesha wote.

Watu wengine waliendelea kulalamika, walikuwa wamechukua miezi 15 na bado hawajafika Kanaani, mahali ambapo ni maili 150 hivi tu kutoka Sinai. Mahali ambapo gari lingechukua ma saa 6 hivi kufika. Walikuwa karibu na nchi ya ahadi lakini mbali kiroho! Ilibidi wabadilishwe kabisa, ili wafae kwenda nchi ya ahadi.

Baada ya hapo Kora, Dathani na Abiramu wakatwaa watu 250 na wakainuka kinyume cha Musa na Haruni. Wakanung'unika kwamba Musa anachukua mamlaka mengi kwamba nao wangepewa uongozi. Musa aliposikia maneno haya akapomoka kifudifudi kisha akanena na Kora na mkutano wote na kuwaambia kwamba asubuhi, "Bwana ataonyesha ni kina nani walio Wake, kisha ni nani aliye Mtakatifu …" Musa alipowaita Dathani na Abiramu wakakataa wakisema amewasumbua kuwa nchi ya maziwa na asali na huku anawaua jangwani, amejikuza mwenyewe awe mkuu juu yao kabisa? "Je! unataka kuwatoboa macho watu hawa? Hatuji." Musa akamwambia Bwana, "sikutwaa punda mmoja kwao, wala sikumwumiza hata mtu mmoja miongoni mwao." Walikuwa wanataka kazi ya

ukuhani, wakaambiwa waje siku inayofuata na watwae kila mtu chetezo cha uvumba na wavilete mbele ya Bwana. Basi wote 250 wakiwa na vyetezo wakaja. "Kora akakutanisha mkutano wote kinyume chao." Utukufu wa Bwana ukatokea mbele ya mkutano wote. Bwana akawaambia Musa na Haruni wajitenge ili awaangamize waovu, ndipo Musa akaanguka kifudifudi na kumsihi Bwana akiwaombea watu wengine waondoke penye hema za waovu ili wasiangamizwe pamoja. Basi nchi ikafunuka, yaani, kama shimo na kuwameza watu hao 250 walioshikamana na Kora na familia zao wakaangamia. Waisraeli wengine wakakimbia kwa woga wasije 'wakamezwa ardhini'. Hiyo ikawa fundisho kwamba makuhani ni wale tu Mungu aliowachagua. Hapa ilikuwa ni ukoo wa Haruni tu.

Siku iliyofuata, watu wakarudia kumlalamikia Musa kwamba ameua watu wa BWANA. Utukufu wa Bwana ukaonekana tena, nao Musa na Haruni wakaanguka kifudifudi kuwaombea watu, lakini tauni ilianza na watu 14,700 wakafa hapo hapo. Musa na Haruni walikuwa na upendo kwa kuwa "walisimama kati ya walio hai na waliokufa, wakimsihi Mungu ili kufanya upatanisho kwa ajili ya watu. Kisha Mungu akataka suala la kugombea kazi ya ukuhani liishe. Akasema wachukue fimbo kumi na mbili na kila moja iandikwe jina la mkuu katika kila kabila na kabila ya Lawi liandikwe jina la Haruni. Akasema, "mtu huyo nitakayemchagua fimbo yake itachipuka, nami nitayakomesha manunguniko ya wana wa Israeli." Siku ya pili Musa alipoingia ndani ya hema ya kukutania alikuta fimbo ya Haruni imechipuka, na kuchanua maua, na hata kuzaa malozi mabivu. Fimbo ya Haruni ikawa ushahidi wa aliyechaguliwa na Bwana kuhudumu, na ikatunzwa Patakatifu pa Patakatifu kando ya sanduku la agano.

Hata leo, tuwe waangalifu kutaka kazi fulani au kugombania kufanya kitu ambacho Mungu alitaka mtu mwingine afanye. Kazi zingine ni za wakfu, na si kila mtu amepewa kuzifanya. Hata hivyo tuwe na roho ya kuridhika. Tusiwe na tamaa kwamba na mimi niwe kama fulani, utauwa na kuridhika ni faida kubwa. Mtu asiyeridhika ni mgumu kuishi naye. Tunaishi wakati ambao watu wana tamaa na wanafikiri nikiwa na kazi hii, au kitu hiki, basi ndiyo nitapata furaha. Wakipata wanavyovitamani wanaona haviwafai, wanavitupa au kuvisahau na kutafuta vingine tena.
Kwa wale walio katika makosa, na wanaostahili kukemewa, hakuna kitu kinachowapendeza zaidi kuliko kupokea huruma na sifa kutoka kwa watu. Watu walipendezwa na Kora aliyedai kuwapenda, nao wakakata kauli kwamba lazima awe mwema, na Musa na Haruni, wabaya. Pia walikuja kujiamini kuwa ni watu wema sana waliodhulumiwa na kunyanyaswa na Musa. Iwapo wangekubali kwamba Kora alikosea na Musa alikuwa sahihi, basi wangelazimika kukubaliana na hukumu kwamba lazima wafe jangwani.

Kora alikuja kuamini kwamba alikuwa mtenda kazi mwenye bidii wa Mungu, na kwamba Mungu alikuwa upande wake. Alijidanganya kwa kufikiri kwamba alikuwa mwadilifu, na kutaniko lilikuwa takatifu. Alijiona kama mtetea haki anayeenda kufanya mabadiliko makubwa katika serikali na kuboresha usimamizi wa serikali ya Musa na Haruni. Musa hakujitetea wala kujilinda, bali daima aliwaombea watu mara kwa mara mbele za Mungu, akitambua ukubwa wa dhambi yao. Tuombe ili tuwe na roho ya unyenyekevu tunapokemewa na viongozi wa Bwana ili tukubali

kurekebishwa na Bwana, tukijua kwamba Yeye anatenda wokovu Wake ndani yetu. Hakika kiburi na tamaa husababisha uasi na maanguko. Uasi unaambukiza! Na inawezekana kabisa kuachana na Uasi! Basi tusiruhusu tamaa ya kile mtu mwingine alicho nacho nasi tusiridhike na kile tulichonacho tayari. tusijaribu kuinua hadhi yetu wenyewe kwa kumshambulia mtu mwingine. Tusitumie sehemu ya Neno la Mungu kusaidia kile tunachotaka, badala ya kuruhusu ukamilifu Wake Mungu kuunda matakwa yetu. Tusitarajie kuridhishwa na mamlaka au cheo. Mungu anaweza kufanya kazi kupitia sisi katika nafasi tuliyo nayo sasa, na wala hatuhitaji kujitukuza. Kila mtu ana ushawishi, na kama wanafamilia, tunahitaji kuwa waangalifu sana ili tusiangamize familia zetu. Badala ya kujiunga na mwanafamilia kufanya maovu, tunapaswa, kwa upendo, upole na hofu ya Mungu kurekebisha makosa yao. Kwa maana tukiungana nao au kukaa kimya, tunaweza pia kuangamizwa pamoja nao. Mungu atusaidie tusiache mashauri na kanuni Zake kamwe, bali tufurahie na kuzifuata hata kama watu wote watakuwa kinyume chetu. Watu walipewa nafasi ya kuchagua upande wanataotaka kuwa. Sisi Leo pia tunapewa fursa za kuchagua upande tunaotaka kuwa, Je, tunataka kumchagua Kristo na kuishi au kumchagua Shetani na kuangamia. Chaguo ni letu!

*Ikiwa watendakazi wetu wote wangekuwa katika hali ambayo wanaweza kutumia saa chache kila siku katika kazi za nje, na kujisikia huru kufanya hivi, ingekuwa baraka kwao; wangeweza kutekeleza kwa ufanisi zaidi majukumu ya wito wao. Kama hawana muda wa kutosha kupumzika, wangeweza kuweka mikakati na kuomba waendelea kufanya kazi kwa mikono yao, na hivyo wangeweza kurudi kwenye kazi yao wakiwa wameburudishwa katika mwili na roho

---

Kwa nini familia za akina Kora waliangamia? Elezea kuhusu fimbo ya Haruni.

**SIKU YA 48**
**( Februari 17)**

# Mungu atoa agizo la kutuma Wapelelezi 12 kwenda Kaanani

**- Hesabu 13-15, 18**

Kama tulivyokwisha kuona, ingechukua wiki mbili tu toka Sinai mpaka Kanani, ambayo ni pungufu ya Kilomita 300, hivyo walikuwa karibu na Kanaani, lakini pia walikuwa mbali mno, kilikuwa ni kitendawili. Walifika mpakani ili waingie Kanaani wakatuma wapelelezi.

BWANA akanena na Musa atume watu 12, mtu mmoja wa kila kabila ili wakaipeleleze nchi ya Kanaani anayotaka kuwapa wana wa Israeli. Watu hawa 12 wawe viongozi, naye Musa akawatuma kutoka nyika ya Parani akawaambia, angalieni "watu wanaokaa kwamba ni hodari au dhaifu … wachache au wengi…" Kama nchi ni njema au mbaya au kuna ngome. Je, kuna unono au njaa, iweni na moyo mkuu mkalete matunda ya nchi." Wakapanda na kwenda huko na ulikuwa wakati wa zabibu, tini na makomamanga. Tawi la zabibu lenye kishada kimoja lilichukuliwa na wanaume wawili. Waliipeleleza nchi siku 40, wakamrudia Musa na Haruni na kumweleza kwamba hakika ni nchi ya "maziwa na asali" na wakaonyesha matunda yake, lakini wapelelezi 10 wakaanza kusifia ukubwa na ushujaa wa watu wa Kanaani na kwamba wao walionekana kama panzi tu wakijilinganisha na wao. Mkutano wote ukapaza sauti na kulia usiku ule na wakaanza manung'uniko tena wakisema, "ingelikuwa heri kama tungelikufa Misri, kuliko katika jangwa hili." Yoshua wa kabila la Benjamini na Kalebu wa kabila la Yuda wakaleta taarifa njema na kuwatia watu moyo kwamba japo kuna majitu kule lakini BWANA kwa mkono wake hodari atawashindia. Wakasema wake zao na watoto wao watakuwa mateka, na hivyo afadhali warudi Misri, basi wakaweka kiongozi awarudishe Misri. Musa na Haruni wakaanguka kifudifudi na Kalebu na Yoshua wakararua mavazi yao, na kusisitiza kuwa nchi ile waliyoipita na kuipepeleza ni njema mno na imejaa maziwa na asali, wakawaambia, "lakini msimwasi BWANA, wala msiwaogope wale wenyeji wa nchi, maana wao ni chakula kwetu naye BWANA yu pamoja nasi, msiwaogope." Japo waliwatia moyo, lakini watu walishika mawe kutaka kuwapiga; ndipo utukufu wa BWANA ukaonekana katika hema ya kukutania mbele ya wote. Bwana akasema,"Je watu hawa watanidharau hata lini? Wasiniamini hata lini? Nijapokuwa nimefanya ishara hizi zote kati yao?"

Mungu akamwambia Musa kuwa atawaangamiza wote na kuwaondolea urithi wao, "Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, kisha lenye nguvu kuliko wao." Musa akamwambia BWANA, Wamisri watasikia hayo, kwamba umewaleta hawa watu kwa uwezo Wako, na kwamba unaonekana uso kwa uso kwa wingu na moto kwa watu hawa, bali hukuweza kuwaleta nchi uliyowaapia na kuwaua nyikani. Musa akamsihi Mungu na kukazia sifa kuu za BWANA, "Si mwepesi wa hasira, mwingi

wa rehema, Mwenye kusamehe makosa…" Musa akamwomba Mungu, "Nakusihi usamehe uovu wa watu hawa." Naye BWANA akajibu "nimewasamehe kama Neno lako lilivyokuwa." Lakini BWANA akasema hawataiona nchi ya Kanaani, bali watatangatanga jangwani kwa miaka 40 ikisimamia siku 40 za kuipeleleza nchi. Alisema, "katika wote walionidharau hapana atakayeiona, bali Kalebu na Yoshua aliyekuwa na Roho nyingine ndani yake, ameniandama wa moyo wake wote. Lakini watoto wao waliohofia kwamba watapata shida "ndio nitakaowaleta na kuwatia ndani, nao wataijua nchi ninyi mliyoikataa." Kweli watoto mna nafasi pia ya kumtegemea Mungu na kumtumaini hata kama wazazi wenu wanafanya yasiyo mema. Alisema "tena watoto wenu mliosema watakuwa mateka na wana wenu wasiokuwa leo na maarifa ya mabaya wala mema, ndio watakaoingia, nao ndio nitakaowapa, nao wataimiliki..."

Hakika ile ripoti ya wapelelezi ilikuwa ya kweli na sahihi. Hawakuwa wakitia chumvi waliposema waliona majitu pale na kwamba wao walionekana kama panzi kwa kujilinganisha. Kosa lao ni katika kuhitimisha kwamba hawawezi kuwashinda watu hao. Hawakuwa na subira ya kutafakari; hawakuamini kwamb Yeyea aliyewafikisha mpaka pale atawapa nchi. hawakukumbuka jinsi Mungu alivyokuwa amewakomboa kwa njia ya ajabu kutoka kwa watesi wao, akikata njia baharini na kuyaangamiza majeshi ya Farao yaliyokuwa yakiwafuata. Walimwacha Mungu nje ya shida yao, na wakatenda kana kwamba ni lazima wategemee tu uwezo wa silaha zao. Je, sisi ni bora kuliko wale wapelelezi kumi katika imani yetu? Yoshua na Kalebu hawakupoteza kamwe mwelekeo wa utume wao, na hawakusahau kamwe yaliyopita—njia yenye kushangaza ambayo Mungu alikuwa amewaongoza kutoka katika utumwa mgumu huko Misri hadi kwenye milango ya Nchi ya Ahadi ilihitaji ujasiri wa kutokubaliana na ripoti za watu kumi walioungana pamoja. Kishawishi cha kuwa mchezaji wa timu huwa na nguvu katika moyo wa mwanadamu. Umoja ni mzuri, lakini kamwe usiwe umoja katika makosa, na kamwe usiwe umoja kwa kuizamisha ile Kweli.

Je, ningetamani kufia Misri kweli? Au ninamtumaini Bwana nikiwa na macho yangu juu ya ahadi Zake? Kuisalimisha mioyo yetu kwenye kutoamini ni kujitumbukiza kwenye mashimo ya adui. Basi tukumbuke kueneza Injili tukiamini Neno hili, ya kwamba Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu."

Kingine cha kukumbuka ni miji ya kimbilio iliyowekwa, nayo ilikuwa safari ya nusu siku kutoka kila sehemu ya nchi, sikuzote barabara zilizoelekea huko ziliwekwa katika hali nzuri. Vibao viliwekwa vyenye neno 'Kimbilio' kwa herufi za wazi, na kwa maandishi yaliyogandamizwa, ili yule anayekimbia asichelewe, yaani achukue muda mfupi kupata hifadhi. Mtu yeyote, yaani Mwebrania, mgeni, au mkazi aliweza kusaidiwa na huduma hii Kesi ya mkimbizi ilipaswa kuhukumiwa kwa haki na mamlaka zinazohusika, na pale tu alipopatikana kuwa hana hatia ya kuua kimakusudi ndipo alipolindwa katika jiji la makimbilio. Wale wenye hatia walikabidhiwa kwa mlipiza kisasi. Wote waliokuwa wametafuta makao katika miji ya makimbilio walikuwa na uhuru wa kurudi kwenye makazi yao kuhani mkuu alipokufa. Msaada huu ulikuwa ni kwaajili ya wale ambao wameua kwa bahati

mbaya, mfano waliweka mbao mahali na hazikuegeshwa vizuri nazo zikaanguka na kumwua mtu. Hakika hayakuwa maisha rahisi kuishi humo, maana mtu aliiacha familia yake kabisa akingoja kuhani mkuu afe! Hakika kilikuwa ni kifungo cha aina fulani. Ila bado ilikuwa ni rehema ukilinganishwa na kuuwawa papo hapo na jamaa za yule aliyekufa. Yaonekana jamii ilitoa msaada fulani wa kuwakimu kimaisha. Miji ya kimbilio ilikuwa ishara ya kimbilio lililotolewa katika Kristo. Mwokozi kwa kumwaga damu Yake Mwenyewe, hakika amewaandalia wahalifu wa sheria ya Mungu mpenyo wa kuponyoka, sote tunaweza kukimbilia humo na kupata usalama kutoka kwenye kifo cha pili. Hakuna nguvu inayoweza kutuchukua kutoka mikononi Mwake sote tunaomwendea kwa kuomba msamaha. Hakuna binadamu asiyehitaji huduma hii "wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, na mshahara wa dhambi ni mauti", Hakuna mwenye haki hata mmoja, haki yetu inatokana na Kristo tu.

Kisha watu wakiwa pale jangwani walimwona mtu akikusanya kuni siku ya Sabato. BWANA aliamuru mtu huyu apigwe mawe kwa sababu ya uasi wa waziwazi ambao wengine wanaweza kuuiga. Hata leo tunaambiwa kutunza siku ya BWANA, siku ya Sabato, si siku ya kujifanyia kazi zetu au anasa zetu. Utunzaji wetu wa Sabato ukoje leo? Je, nyakati fulani tunasahau kwamba Mungu anapendezwa na mambo madogo na makubwa na hatakubali ibada yenye uzembe? Wengine wanaidharau Sabato leo na wamejichagulia siku tofauti. Wengine, ingawa wanaitambua Sabato, wanashindwa kuitakasa kwa kutojitayarisha vya kutosha kwa ajili yake. Wengine huchagua kusema maneno yao wenyewe au hata kufanya mapenzi yao wenyewe, hivyo wanashindwa kuweka wakfu siku hiyo kwa Mungu. Hebu tuombe Mungu atuumbie mioyo safi leo.
Mashauri kama yatakuwa msaada kwako

NJIA ZA MSAADA KATIKA UTUNZAJI SAHIHI WA SIKU YA BWANA.
1. Siku ya BWANA huanza wakati wa jioni na kumalizika jioni wakati wa jua kuzama, hivyo basi, kupika, kusafisha nyumba, kufua, kunyoosha nguo, na kazi nyingine zote za kawaida zinatakiwa kuwa zimemalizwa kabla ya Siku ya BWANA kuanza. Kubadilika kwa siku usiku wa manane kulifanywa na warumi, lakini siku mpya ya Mungu huanza jua linapozama hadi jua linapozama tena siku, soma zaidi kuhusu hili. Ifanye Sabato iwe siku ya pekee kwa kuandaa chakula maalum, na vitu vya kufanya kwa ajili ya familia yako. SomazZaidi na waulize wengine wakupe mawazo zaidi ikawa wanatamani Sabato iishe ili "wajiachie". Omba upate mafunuo toka kwa Mungu maana hayaji kirahisi! Kama unaweza kufanya shughuli nyingine za kifamilia kwa furaha, acha Siku ya BWANA iwe ya maandalizi na tafakari. Siku hii imeitwa Sabato katika Maandiko Matakatifu na katika lugha zaidi ya mia moja duniani.

2. Ni sahihi siku ya BWANA kupasha chakula chako ulichopika siku ya Ijumaa.

3. Ingekuwa vyema kujiepusha na vitabu vingine vyote vya kidunia, majarida, magazeti, mtandao wa internet, Iphone, Redio, vipindi vya televisheni ama mambo yote yahusikayp na teknelojia, n.k mpaka Siku ya BWANA itakapoisha.
4. Miamala ya kibiashara kama Benki, malipo ya kodi, migahawa, kununua gesi,

kununua magazeti, kuuza maziwa,barafu n.k vinatakiwa kusubiri mpaka masaa ya Siku ya BWANA yameisha, ambayo humaanisha jioni ya Jumamosi baada ya jua kuzama. Jaribu “kutosimama langoni” kama walivyofanya kipindi cha Nehemia, wakisubiri Siku ya BWANA iishe ili kwamba wauze bidhaa zao. Kwa ufupi usikope siku moja ya Mungu, wakati ambapo amekupatia siku sita kufanya kazi zako.

5. Sherehe, Mikusanyiko ya kijamii, na shughuli nyingine za kidunia kama makundi, nyimbo zote, Tennis n.k kamwe isingeruhusiwa katika Masaa matakatifu.

6. Siku ya BWANA ni muda mzuri kwa vijana na watu wazima mchana kutembelea tembelea viumbe vya asili na kujifunza juu ya mimea na maisha ya wanyama. Si vyema kubadili muda wa ushirika wa kanisa na maburudisho ama kutembelea viumbe vya asili. Masaa ya Siku ya BWANA ni muda mzuri pia wa kutembelea waliofungwa na waliolazwa hospitalini. Kutembelea wagonjwa, wafiwa ama wafungwa wakati wa muda wa Ibada, inatakiwa kufanyika kwa nadra sana labda tu kama jambo la dharura ama tukio mahususi. Nenda huko ukaweke ibada au fanya baada ya ibada. Ni rahisi kupata jotojoto kwenye ushirika na wenzio na unaweza kujenga ushirika na watu hao baada ya hapo. Nadhani, mifano tuipatayo katika Biblia, yaonyesha Yesu hakuahirisha kwenda kusali kwa sababu alikuwa anaenda kumuona mgonjwa. Aliendelea kufanya hivyo muda wote baada ya Ibada kanisani. Bila shaka “ hakukopa muda wa Kanisa”

7. Sabat0 ni muda mzuri wa kujifunzakila juma kuhusu siku ya BWANA mchana, wewe na familia yako na kama ikiwezekana shiriki katika michezo ambayo itakuza mahusiano yako na Mungu (Michezo ya Biblia).

8. Mungu hufurahishwa tunapojitenga mbali si tu na kazi, lakini pia katika kujiepusha kuzungumza maneno yetu na kuwaza mawazo yetu siku ya BWANA. Hili ni gumu lakini omba kwani ni jambo ambalo mafarisayo walikuwa na shida nalo, matendo yao yalikuwa sahihi, lakini dhamira, mawazo na tabia zao walikuwa mbali mno. Najikuta mara kadhaa nikiwa nafuta koki za bafuni ama kuondoa utando wa buibui bila kufikiri kuwa ni Sabato.

9. Tunaonesha dharau kwa Mungu, tunapoamua kulala masaa yote ya Sabato na kujitenga na Ibada katika nyumba ya Mungu (japo si dhambi saa moja ama mawili siku ya Sabato mchana, ila kulala siku nzima ili kwamba usome usiku, ama upate nguvu za kufanya mambo  yako baada ya Siku ya BWANA si njia sahihi.

10. Tunamheshimu Mungu kwa kukusanya familia yetu pamoja, tukiimba kwa mtizamo wa Ibada wakati wa kufungua na kufunga Siku ya BWANA.

*Ombi la Kweli au dhati Halitegemei Wakati au Mahali au Hali—Omba chumbani mwako au mahali pa faragha, na unapoendelea na kibarua chako cha kila siku, acha moyo wako uinuliwe kwa MUNGU mara kwa mara.


---------------

Kutoka Misri mpaka Kanaani kwa mguu ni wastani wa muda gani? Kwa nini watu walilia machozi waliposikia ripoti ya watu kumi? Kuna umuhimu gani kwetu kutoa ripoti njema za wema wa Mungu? Kwa nini aliyekuwa anakusanya kuni siku ya Sabato aliuwawa? Je, unawajua Shamua, Shafati, Igali, Palti, Gadieli, Gadi, Amieli, Sethuri, Geueli, na Nabii? Kama hujawahi kuwasikia, ni kwa sababu gani?

**SIKU YA 49**
**( Februari 18)**

# Maji ya Meriba Yamfanya Musa Asiingie Kanaani

**- Hesabu 20 na 21**



Waisraeli walizunguka jangwani miaka 40 wakifundishwa na Mungu kumtumaini na kumtegemea. Hayajaandikwa mengi ya miaka hii 40, tuna imani mioyo yao ilipondeka na maisha haya magumu yalikuwa mshahara wa kutomtumaini Mungu na kuendelea na malalamiko. Hata hivyo Mungu hakuwaacha, aliendelea kuwaongoza akiwapa riziki zote za kila siku, iwe mana, maji, nguo au pa kulala. Siku moja wakizunguka jangwani walifika Kadeshi. Hapa ndipo Miriamu alipokufa na kuzikwa. Lakini pia hapakuwa na maji. Watu wakajikusanya na kushindana na Musa, na kusema ni heri wangekufa kule ndugu zao walipokufa. Wakalalamika wakisema, hapa hapana zabibu, tini wala makomanga au maji ya kunywa. Musa na Haruni ambao walikuwa bado wanamwombolezea dada yao walianguka kifudifudi na utukufu wa BWANA ukatokea. BWANA akamwambia Musa atwae fimbo na akauambie mwamba mbele ya macho ya watu utoe maji. Lakini Musa akiwa na hasira, alisema "sikieni sasa enyi waasi, Je, tuwatokezee maji katika mwamba huu?" Badala ya kuzungumza na mwamba kama alivyoambiwa akainua mkono wake na kuupiga ule mwamba mara mbili. Mwamba uliopigwa ulimwakilisha BWANA Mwenyewe. BWANA akamwambia Musa na Haruni, "kwa kuwa hamkuniamini Mimi, ili kunistahi mbele ya macho ya wana Israeli," hamtaingia nchi ya Kanaani. Maji haya ya Kadeshi yakaitwa maji ya Meriba, kwa sababu wana wa Israeli waliteta na Bwana.

Waisraeli wakampelekea habari mfalme wa Edomu ili awape ruhusa wapite katika nchi yake wakiwa safarini lakini akakataa. Kisha BWANA akanena na Musa akamwambia kuwa umefika wakati wa Haruni kupumzika kwa kulala mauti kwa kuwa asingeingia Kanaani kwa sababu waliasi kinyume cha Neno Lake penye maji ya Meriba. Basi Eleazari kijana wake mkubwa na Musa wakapanda mlima wa Hori

na Musa akamvua kaka yake Haruni mavazi ya Ukuhani na kumvika mtoto wake Eleazari. Haruni alikuwa anaenda kupumzika, na ilikuwa wakati wa Eleazari kuchukua jukumu hilo! Kaka wawili wakaangaliana na kuagana. Basi Haruni akafa huko kilele cha mlima Hori, akiwa na miaka 123, watu wakamwomboleza kwa mwezi mmoja. Japo walikuwa wamemsumbua na kushindana Naye, sasa walitambua wema Wake.

Kisha wakasafiri wakiizunguka nchi ya Edomu. Kwa vile hawakuruhusiwa kukatisha pale, watu wakaanza kulalamika tena kwamba hapana chakula, kwamba Musa anataka wafe jangwani bila maji, na kuhusu mana walisema, "roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu." BWANA akatuma nyoka wa moto na wakafa watu wengi. Musa akawaombea watu na BWANA akamwambia Musa atengeneze nyoka wa shaba na amweke juu ya mti, hata "itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi." Musa alitengeneza nyoka wa shaba, akamtundika kwenye mti, hata ikiwa nyoka alimwuma mtu, alipomtazama yule nyoka wa shaba aliishi. Waliokataa kumwangalia nyoka wa shaba kwa ukaidi, au wakifikiri "hili litawasaidia nini", walikufa. Hata leo, Maagizo ya Mungu ni muhimu, hata kama tunafikiri tunajua sana, utii ndiyo muhimu kuliko kila kitu, kuitii sauti ya Mungu wetu. Yesu alirudia kisa hiki cha nyoka kwa Nikodemu katika injili ya Yohana na kwa watoto au watu wote. Somo la kumtegemea Mungu na Neno Lake, "kama vile Musa alivyomwinua Nyoka jangwani, vivyo hivyo mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika Yeye". Basi pale penye kila weka jina lako wewe.

Si nyoka wa shaba aliyewaponya watu, bali Mungu, kwa njia ya imani. Leo, unapoumwa na Shetani, mwangalie Yesu kwani kila amwaminiaye, hatapotea bali atapata nguvu za milele.

*Hakuna wakati au mahali ambapo haifai kutuma ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika roho ya maombi ya bidii. Katika msongamano wa watu mitaani, katikati ya biashara au shuguli, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kusihi mwongozo wa MUNGU, kama vile Nehemia alipotoa ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu na faragha unaweza kupatikana popote tulipo. Mara zote tunapaswa kuacha mlango wa moyo ukiwa wazi na kutuma mwaliko wetu kwenda juu ili Yesu aje akae nasi kama mgeni kutoka mbinguni kwenye nafsi zetu

---

Kwa nini Musa alihesabiwa dhambi penye maji ya Meriba? Kwa nini alifanya dhambi? Kwa nini Waisraeli hawakupitia Edomu? Nyoka wa shaba aliwakilisha nani? Nani alishika kazi ya Haruni baada ya kifo chake? Yesu anarudiaje kisa cha nyoka jangwani?

**SIKU YA 50**
**( Februari 19)**

# Safarini na Changamoto Zikiendelea

**- Hesabu 21-26**



Waisraeli wakiwa wanaendelea na safari katika kitabu hiki tunaona kwamba waliumwa na nyoka kule jangwani. Na wakapata tiba. Sote tumeumwa na nyoka aitwaye Shetani. Sumu ni dhambi. Isipokuwa tuutazame msalaba na kuukazia macho, tutaangamia. Hivyo, tusiondoe macho yetu msalabani! Kwa kupata wokovu, tuutazame msalaba. Maafa yanapotokea, tuutazame msalaba. Tunapokata tamaa, tuutazame msalaba. Tukiwa na uchungu, tuutazame msalaba na tumwone Muumba wetu asiye na dhambi akiugua kwa maumivu kwa ajili yetu. Shime, tuuangalie msalaba, daima!

Waisraeli walikuwa wamekaa utumwani Misri, kisha jangwani bila vita. Pengine jangwani walijifunza kumtegemea Mungu na kuwa na umoja ili Mungu awapiganie. Basi Waisraeli wakafika nchi ya Waamori, na wakamwomba Sihoni mfalme wao awaruhusu kupita kwa amani bila kuingia kwenye mashamba yake wala kunywa maji yake visimani. Lakini Sihoni hakukubali kuwaacha wapite katika mpaka wake, bali akataka kufanya vita nao. Alipotoka ili kupigana na Israeli jangwani, alipigwa vikali karibu na mto Yaboki, pale Yakobo alipoomba usiku kucha, na Israeli ikatwaa miji yake yote na kukaa hapo, huo ulikuwa ushindi wao wa kwanza. Wakaendelea kwa Ogu mfalme wa Bashani. Wakaomba ruhusa wapite, walisema “hatutageuka kando kwenda mashambani, wala kuingia katika mashamba ya mizabibu, hatutakunywa maji ya visimani; tutakwenda kwa njia kuu ya mfalme hata tutakapokuwa tumepita mpaka wako.” Lakini Ogu naye hakuwaruhusu bali alitoka apigane na Israeli lakini naye alipigwa pamoja na watu wake na nchi yake kutwaliwa.

Kisha wakaingia tambarare ya Moabu ng’ambo ya pili ya Yordani, karibu na Yeriko. Ndipo Balaki mwana wa Sipori aliyekuwa mfalme, akijua mambo ambayo

Mungu alikuwa amewatenda Waamori na wafalme Ogu na Sihoni, akaogopa sana na watu wake wa Moabu. "Jeshi hili la watu litaramba vitu vyote vinavyotuzunguka, kama vile ng'ombe arambavyo majani ya mashamba". Akakazana kutafuta wachawi wawakomeshe waisraeli maana alijua wanaongozwa na Mkuu zaidi yake. Akamwita Balaamu aliyekuwa nabii wa Mungu wa mbinguni atoe unabii. Naye Balaamu akatabiri, "Tazama wanaufunika uso wa nchi, tena wananikabili mimi, basi njoo wewe, nakusihi unilaanie watu hawa, maana wana nguvu kunishinda mimi. Labda nitawaweza, tupate kuwapiga, niwafukuze kutoka nchi yangu kwa maana yeye umbarikiye hubarikiwa naye umlaaniye hulaaniwa." Hakujua kwamba Mungu Ndiye aliyempa uwezo wa kubariki na kulaani. Wazee wa Moabu na Midiani wakaenda na ujira na uganga mikononi mwao kwa Balaamu na kumpa ujumbe toka kwa mfalme Balaki. Balaamu akijua kabisa kwamba Israeli anaongozwa na Mungu aliwaambia wakae pale usiku ili apate jibu toka kwa Bwana.

Mungu akamtokea Balaamu na kumwambia ni watu gani wamo nyumbani mwake. Akajijitea kwamba Balaki mfalme wa Moabu amewatuma kwake akiwaogopa Waisraeli. Mungu akamwonya Balaamu asiende na watu hawa wala asiwalaani Waisraeli kwani wamebarikiwa. Balaamu aliwaambia wale wazee asubuhi waende kwao maana "BWANA amekataaa kunipa ruhusu kuondoka pamoja nanyi kwenda kwa Balaki." Wakuu walipeleka ujumbe kwa Balaki naye akatuma watu wengine wenye cheo kuliko wale wa kwanza nao wakamfikia Balamu kumwomba aende na akamsihi kwamba neno lolote lisimzuie huku akimwahidi akisema "maana nitakufanyizia heshima kubwa sana na neno lolote utakaloliomba nitalitenda." Akakazana nabii huyu alaani watu hawa. Naye Balaamu akasema hata kama Balaki angempa nyumba imejaa fedha na dhahabu, hawezi kuongeza au kupunguza lile Neno ambalo BWANA anataka aseme. Japo alijua ni makosa, alikuwa na tamaa ya zawadi za mfalme na kuwasihi wale watu wakae tena usiku ule. Ndipo Mungu alipomtokea tena Balaamu na kumwambia kwa vile anakazana sana kuwa na watu hao, aende nao tu lakini akamwambia, Neno lile nitakalokuambia Ndilo utakalolitenda." Balaamu aliondoka asubuhi na kupanda punda, ndipo hasira ya BWANA ikawaka kwa sababu ya ukaidi wake wa kwenda, na Malaika wa BWANA akajiweka njiani ili kumpiga akiwa amepanda punda na watumishi wake wawili pamoja naye. Punda alimwona Malaika na upanga Wake mkononi, na punda akageuka upande kuiacha njia, akaingia shambani. Balaamu alimpiga punda ili kumrejeza njiani, ndipo Malaika wa Bwana akaenda kusimama mahali pafinyu ambapo wasingeweza kupita. Yule punda, alipomwona malaika wa BWANA tena akajilaza chini na Balaamu kwa hasira akampiga punda kwa fimbo yake. BWANA akakifunua kinywa cha punda na akanena "nimekutenda nini, hata ukanipiga mara tatu hizi." Balaamu bila kufikiri akaanza kujibishana na punda, bila hata kushangaa mnyama anayezungumza. Akaona ameshushwa hadhi mbele ya wageni wake na watumishi, akajibu bila kufikiri kwamba anazungumza na punda akisema, "kwa sababu umenidhihaki, laiti ningekuwa na upanga mkononi mwangu ningekuua sasa hivi". Punda akamkumbusha kwamba yeye ni punda wake wa muda mrefu na amekuwa mwaminifu na sasa Balaamu amempiga mara tatu. BWANA akafungua macho ya Balaamu na akaona Malaika amesimama na upanga uliofutwa mkononi Mwake, Balaamu akainama kichwa na kuanguka kifudifudi. Malaika wa BWANA akamwuliza kwa nini amempiga punda wake; akamweleza Baalamu kwamba alikuja

kumpiga yeye kwa vile njia yake imepotoka na isingekuwa punda wake angelimwua yeye na kumwacha Punda. Balaamu akaomba msamaha "nimefanya dhambi…" Akakiri kwamba hakujua ya kuwa Malaika amesimama njiani ili kumpinga. Akasema kwamba atarudi ikiwa yule malaika amechukizwa. Alikuwa anasema tu, bali moyoni alitaka sana kwenda ili 'apokee rushwa' na kusema neno baya kwa Israeli. Malaika akaona kama anasisitiza na kumwambia aende tu, bali neno lile atakaloambiwa na BWANA Ndilo aliseme. Mara nyingi nasi tunalazimisha matakwa yetu, na BWANA anatupa uchaguzi, kisha tunaenda na kuangamia.

Katika Biblia, kuna wanyama wawili tu waliowahi kuzungumza, nao ni nyoka na punda wa Balaamu na yote yalikuwa ni kengele ya kuashiria mambo fulani. Kisa hiki pia kinatutahadharisha kujali kutunza na kuwa na huruma na viumbe wa Mungu. Mungu alikuwa tayari kumwua Balaamu bali kumponya punda aliyekuwa tayari kutii sauti ya Mungu. Mungu hana upendeleo hata kwa nabii anayekiuka sauti Yake.

Balaki alienda kumlaki Balaamu aliposikia amefika Moabu. Balaki akasema alitaka ampe heshima na zawadi nyingi, mbona hakuja? Balaamu akamwambia kuwa amekuja ila atasema tu lile Mungu atakalomwambia. Mgeni huyu aliwasili na hatimaye walienda mahali pa juu pa Baali na akawaona wana Israeli kutokea mlima huu. Balaamu akamwambia Balaki afanye madhabahu ili watoe kafara, naye alifanya. Basi Balaamu alipoanza kutabiri hakuweza kuwalaani Israeli. "Nimlaanije yeye ambaye Mungu hakumlaani? Nitamshutumuje, yeye ambaye BWANA hakumshutumu?" Balaki alikasirika kwamba ameletwa kulaani na hafanyi kazi hiyo. Alifikiri kuwa nabii wa Mungu anaweza kusema kitu cho chote apendacho. Mfalme aling'aka 'analipwa' bali anawabariki zaidi adui zake. Balaamu akajibu kuwa imempasa kusema Neno la Mungu. Basi madhabahu yakajengwa na sadaka ya kuteketezwa ikatolewa, na Baalamu akapata Neno toka kwa BWANA "Mungu si mtu aseme uongo; wala si mwanadamu ajute" akaendelea kuwabariki Waisraeli mpaka Balaki akasema "usiwalaani wala usiwabariki! Balaamu alisikitika kukosa zawadi. Wakaenda kilele cha Mlima Peori na kujenga madhabahu na kutoa kafara tena. Mungu akamjia na akaanza kubariki Waisraeli tena, "mahema yako ni mazuri namna gani, Ee Yakobo, maskani zako Ee Israeli…maji yatafurika katika ndoo zake. Mungu amemleta kutoka Misri, ana nguvu mfano wa nguvu za nyati, atawameza mataifa walio adui Zake, ataivunja mifupa yao vipande vipande, atawachoma kwa mishale yake … na abarikiwe kila akubarikiye, na alaaniwe kila akulaaniye." Balaki akapiga makofi ya hasira na kumwambia kwamba amemwita amlaanie adui zake na mara tatu hizi anawabariki basi akamfukuza atoke aende kwake "naliazimu kukuheshimu sana; lakini tazama, BWANA amekuzuilia heshima.

Balaamu alipata maono ya unabii wa kuzaliwa kwa masihi, alisema "namwona, lakini si sasa; namtazama, lakini si karibu; nyota itatokea katika Yakobo na fimbo ya enzi itainuka katika Israeli… Mtawala atakuja kutoka Israeli…" Unabii huu ni katika unabii wa kuzaliwa kwa Masihi, aliyetoka katika ukoo wa Yakobo na kisha Yuda na familia za kifalme kama mfalme Daudi na Sulemani.

Balaamu ambaye alikuwa mtumishi wa mshahara tu, alipanga njama mbaya sana baadaye kule Shitimu au Baal-Peori na kufanya wanaume wa Israeli wachukue wanawake wa Moabu na kuingia katika kuabudu miungu ya Baali. Kwa kuoa wake kule, walipunguza nguvu yao kabisa. Hili lilifanya Waisraeli 24,000 kufa kwa siku moja. Kuhani Finehasi akawaua viongozi wa jambo hili nao walikuwa ni mwanamke Kozbi Mmoabi na Zimri, mwanamume Mwisraeli na kufanya pigo hili likome. Kutii sauti ya Mungu ni muhimu sana.

Ingekuwa heri Balaamu angekaa nyumbani na kukataa Balaki alipomwita, au kurudi alipomwona malaika, angeishi kwa heshima. Japo alijua mapenzi ya Mungu lakini aliendа kinyume na kufa pasipo matumaini katika nchi ya watu wasiomjali Mungu.

*Popote tulipo, bila kujalisha kazi yetu au taaluma ni nini, mioyo yetu inapaswa kuinuliwa kwa MUNGU katika maombi. Hii ni kuwa na utayari katika maombi wakati wowote. Hatuhitaji kusubiri hadi tuweze kupiga magoti kabla ya kuomba. Wakati fulani, Nehemia alipofika mbele ya mfalme, mfalme aliuliza ni kwanini alionekana kuwa mwenye huzuni, na ni ombi gani alikuwa anataka kutoa kwa mfalme. Lakini Nehemia hakuthubutu kujibu hapo hapo. Masilahi muhimu yalikuwa hatarini. Hatima ya taifa ilining'inia juu ya mtazamo ambao unapaswa kutengenezwa juu ya akili ya mfalme; naye Nehemia akatuma maombi kwa MUNGU wa Mbinguni, kabla hajathubutu kumjibu mfalme. Matokeo yakawa kwamba alipata yote aliyoomba au hata kutamani.


---

Taja majina ya wafalme wawili waliopigwa na Israeli? Kwa nini si vyema mtu wa Mungu kutamani mali au rushwa? Je, ungesikia punda anazungumza ungefanya nini? Balaki alisemaje kuhusu Masihi? Kwa nini watu 24,000 walikufa? Kwa nini ingekuwa bora kama Balaamu angebaki nyumbani tu? Lipi ni bora, kuheshimiwa na Mungu au Balaki?

**SIKU YA 51**
**(Februari 20)**

# Matoleo na Sikukuu na Kuhesabiwa kwa Waisraeli

**- Hesabu 26-31**



Hatimaye mwisho wa nabii aliyetaka kutumiwa na watu ili apate mali badala ya kutumiwa na Mungu uliwadia. Israeli sasa walikuwa wamepiga kambi mashariki mwa mto Yordani, wakitazamana na Yeriko. Hapa wakapewa amri ya kuhesabu wanaume wote ambao wanaweza kuwa jeshini, yaani, kuanzia umri wa miaka 20. Miaka 40 iliyopita walipohesabiwa, wanaume wa umri huo walikuwa 603,550 na sasa walikuwa 601,730. Sensa hii inatuonyesha kuwa idadi ilikuwa imepungua, kwa kuwa nchi yoyote ikifanya sensa baada ya miaka 40 inategemewa watu waongezeke. Mfano Tanzania watu walipohesabiwa mwaka 1969 walikuwa milioni tisa na mwaka 2022 walikuwa milioni 63. Mungu huorodhesha majina mara kwa mara kwa sababu watu ni muhimu Kwake. Yeye aonaye shomoro akianguka na anayejua idadi ya nywele kwenye kichwa chako Analijua jina lako na kila kitu kukuhusu wewe, na yote ni muhimu Kwake. Mbinguni kuna kitabu kiitwacho Kitabu cha Uzima (Ufunuo 20:12). Ndani yake humo kuna majina yote ya wale ambao wataokolewa milele. Swali kuu la kujiuliza ni "Je! Jina langu limeandikwa humo?" Leo, kwa nini usizungumze na Bwana? Muombe akusamehe na akuokoe. Kwa furaha, Yeye ataongeza jina lako kwenye orodha Yake!

Wakiendelea na kuhesabu watu, mabinti wa Selofehadi mwana wa Heferi wa kabila ya Manase mwana wa Yusufu walipanga kuonana na Musa, majina yao yalikuwa Mala, Noa, Hogla, Milka na Tirsa. Wakasimama mbele ya Musa na wakuu mlangoni pa hema ya kukutania, wakasema baba yao alikufa nyikani naye hakuwa na mwana wa kiume, na wao waliona kwamba jina la baba yao litafutika katika jamaa zake kwa vile hakuwa na mwana wa kiume. Kwa ujasiri wakaomba "Tupe sisi urithi pamoja na ndugu zake baba yetu". Jambo ambalo lilikuwa gumu siku hizo, ila wasichana hawa walikuwa mashujaa. Pengine walichagua mmoja awe msemaji ili wasiingiliane wakati mwingine akizungumza. Musa akaleta hili neno mbele za Bwana. Bwana akamwambia Musa kwamba binti hawa wananena lililo haki, "kweli utawapa miliki ya urithi pamoja na ndugu za baba yao; nawe utawapa

urithi wa baba yao." Bwana anajali kila jambo la maisha yetu. Mungu akamwambia Musa kuwa mtu akifa naye hana mwana wa kiume "ndipo utampa binti yake urithi wake. Tena ikiwa hana binti mtawapa nduguze urithi wake. Na ikiwa hana ndugu, mtawapa ndugu za babaye huo urithi wake…" Neno hili likawa Amri na hukumu kwa wana wa Israeli kama Bwana alivyomwagizia Musa. Zile tamaduni ambazo zina shida na jambo hili, huu ni mfano wa kuiga.

Mabinti hawa waliolewa baadaye na watu wa kabila la baba yao, ili urithi ubaki kwenye kabila hilo. Walifanya historia ambayo iliwabariki mabinti wengine wa siku za baadaye. Hata hivi leo, ni vizuri kufuata hii Sheria Mungu aliyoitoa.

Mungu alirudia maagizo mengine aliyokuwa amemwambia Musa, mfano, matoleo ya sadaka, jinsi ya kutunza nadhiri kwa Mungu na Amri Zake. Mungu akamwambia Musa ajiandae kulala mauti katika mlima wa Abarimu. Lilikuwa jambo gumu kulikubali na yote yalitendeka kwa dhambi moja kwenye maji ya Meriba. Dhambi ya Musa ilikuwa ni ipi? Musa alikuwa amewakasirikia watu "Lakini Mimi nawaambia, Yeyote atakayemkasirikia ndugu yake atahukumiwa." Kisha Musa akasema "Sikieni sasa, enyi waasi; je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu?" Mungu pekee Ndiye angeweza kuleta maji kutoka kwenye mwamba. Musa Alikuwa ameuchukua Utukufu wa Mungu na Akaupiga mwamba mara mbili, badala ya kuzungumza tu. Mwamba ulimwakilisha Kristo, atakayekufa mara moja na si mara mbili. Katika kazi zetu zote za huduma Kwake, lazima tuwe waangalifu tusiwafanye watu waamini kuwa sisi ndiyo wenye uwezo wa kutenda. Heshima na utukufu vinapaswa kutolewa kwa Mungu kila wakati kwa jambo lolote lile jema tunalofanya. Mungu Ndiye aliyekuwa kiongozi na Mpaji katika safari. Haruni naye alikaa kimya alipomwona Musa akifanya makosa. Mungu alihesabu ukimya wa Haruni kama uasi (Hes. 20:24). Musa Alikuwa amefikisha miaka 120, alikuwa amewaongoza Israeli kwenye yote, iwe ni vita au mashauri. Mungu ni mwema, na mashauri Yake siku zote ni mazuri kwetu japo hatuyaoni. Musa akaachia uongozi kwa Joshua (Hoshea) mwana wa Nuni na akamweka mbele ya Eleazari kuhani na mbele ya mkutano wote, kisha Eleazari akaweka mikono yake juu ya Yoshua, na akampa mausia kama Bwana alivyosema kwa mkono wa Musa.

Mara ya mwisho ulihudhuria mkutano wa makambi lini? Suraya 28 na 29, inarudia maagizo ya jinsi ya kusherehekea baadhi ya hafla ambazo zimetolewa kwanza kwenye kitabu cha Mambo ya Walawi (Mambo ya Walawi 16, 23 nk). Tamasha tatu za kila mwaka zimeelezewa hapa:

1. Sikukuu ya Baragumu (Hesabu 29: 1-6): Hili lilikuwa tukio la siku moja ambalo lilifanyika siku ya kwanza ya mwezi wa saba wa Kiyahudi. Tarumbeta zilipigwa siku hiyo na ikatunzwa kama Sabato. Sadaka ya kuteketezwa, sadaka ya unga, na sadaka za dhambi zilitolewa kwa BWANA. Sikukuu hii iliwatayarisha Waisraeli kwa Siku ya Upatanisho iliyofuata.

2. Siku ya Upatanisho (Hesabu 29:7-11): Hii ilifanyika siku kumi baada ya sikukuu ya baragumu. Siku hii ndiyo ambayo Patakatifu palitakaswa kwa kutoa dhabihu zifaazo.

3. Sikukuu ya Vibanda (Hesabu 29:12-40): Hii ilikuwa sikukuu ya mwisho ya mwaka. Zilikuwa siku saba za sherehe zenye furaha. Dhabihu zinazopaswa kutolewa kila siku zimefafanuliwa hapa. Sikukuu hizi za kila mwaka husaidia kuelekeza uangalifu wa Waisraeli kwa Mungu, na kuwaleta karibu na Mungu. Kimsingi, tulichonacho sasa ni mkutano wa mwaka wa makambi ambao ukiendeshwa vyema, unaweza kuwaasha na kuwaletea matengenezo wale waliohudhuria. Ikiwa mna makambi katika sehemu yenu ya dunia, tafadhali usikose mkutano wa makambi mwaka huu. Baraka zinakungoja hapo!

Musa akaandika jinsi walivyosafiri, kwa amri ya BWANA na ndiyo maana leo tuna kumbukumbu ya Safari ya wana wa Israeli. Safari yetu duniani sasa ni kama ya wana wa Israeli, kwani tu katika utumwa wa dhambi, na kila siku Mungu anatuongoza. Si kwa wingu na moto kama zamani bali kwa Neno Lake na Roho Wake ili tufike mbinguni au ile Kanaani mpya. Wapenzi watoto tuombe kusikia sauti Yake tusije kuwa kama Waisraeli waliotoka Misri lakini wakaangamia jangwani. Kwa saburi tujenge imani yetu, kumtegemea Mungu na kuitii sauti Yake.

*

Tukumbuke dhabihu ambayo Yesu aliitoa. Unapofikiria wana-kondoo wote waliotolewa dhabihu, hakika ulikuwa mpango wa gharama kubwa kuwakumbusha waabudio kwamba wokovu unakuja kwa gharama isiyo na kikomo. Mwana-Kondoo wa Mungu alikuja kama zawadi kuu zaidi ya mbinguni, akionyesha kikamilifu zaidi kuliko wakati mwingine wowote upendo usio na kipimo wa Mungu. Tumekombolewa kwa huruma Yake isiyo na kifani, Sisi ni watoto wake. Nasema, Haleluya! Na wewe Je? Chukua muda leo kufikiria juu ya njia ambazo dhabihu ya Yesu pale Kalvari inaathiri maisha yetu. Hakika Yeye Ametuletea tumaini na amani, Amerejesh amahusiano yetu yaliyovunjika na Mungu na watu wengine, na anataka kuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku kama chakula tunachokula kila siku. Yeye Ndiye dhabihu yetu kamilifu.

*Madhumuni yako yote mema na dhamira njema havitakuwezesha kustahimili mitihani ya majaribu. Lazima muwe watu wa maombi. Maombi yenu hayapaswi kuzimia, kuwa ya msimu yaani, hapa na pale bila kanuni, na ya mihemko, bali ya bidii, ya dhati, ya kudumu, na ya mara kwa mara (au daima). Sio lazima uwe peke yako, au upige magoti kuomba; lakini katikati ya shuguli zenu, nafsi zenu zinaweza kuinuliwa mara kwa mara kwa MUNGU, zikishikilia nguvu Zake; ndipo mtakapokuwa watu wa kusudi la juu, bora, takatifu, na waadilifu ambao hawatageuzwa kwa namna yoyote kutoka katika ile Kweli, na njia sahihi , na haki.

---

Nani walichaguliwa kuchukua nafasi ya Musa na Haruni? Je, Waisraeli jangwani walikuwa na Maandiko ya Torati? Kwa nini tumepewa Maandiko? Chukua namba ya wanaume toka Misri na utoe ya wale wanaume waliohesabiwa baadaye, tofauti ni ngapi? Kwanini ni muhimu kuhudhuria makambi?

**SIKU YA 52**
**(Februari 21)**

# Kitabu cha Kumbukumbu la Torati - Kisa kinarudiwa mara ya pili wakati Musa anaaga Jeshuruni

Kabla ya Musa kufa ng'ambo ya mto Yordani katika Araba aliwaambia maneno ambayo yaliandikwa kwenye kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Alirudia yale ambayo waliyapitia kwenye vitabu vinne vya kwanza baada ya kumpiga Sihoni mfalme wa Waamori na Ogu mfalme wa Bashani. Aliwakumbusha kwamba, BWANA Mungu amewafanya kuwa wengi na amewawekea nchi mbele yao ili wakaingie na kuimiliki kama alivyowaapia Baba zao Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Musa akasema yeye hataweza kuwachukua peke yake, bali BWANA Mungu anaweza Naye amewabariki na kuwafanya wawe mfano wa nchi zote duniani. Walikumbushwa kutoabudu sanamu za kuchonga. Ibada ya sanamu ni uovu mbele za BWANA. Hata leo watu wengi wana miungu mingine. Yaweza ionekane au isionekane. Miungu hii yaweza kuwa michezo yetu, matumbo yetu au chakula, michezo ya kompyuta, televisheni, hirizi, maoni, fasheni, urembo, nyumba, familia, marafiki zetu au cho chote kile ambacho tunakipatia kipaumbele kuliko Mungu. Bwana Ndiye Mungu na hapana mwingine duniani wala mbinguni, ni YEYE peke



Yake anayestahili sifa na kuabudiwa. Akawaambia mambo ya siri ni ya BWANA Mungu, ila yale aliyofunua ni ya waumini wote na watoto wao, ili waweze kuyatenda. "Akawaambia, Yawekeni mioyoni mwenu Maneno yote ambayo nashuhudia kwenu hivi leo; nayo waamuruni watoto wenu, wayatunze na kuyafanya maneno yote ya torati hii. Kwa maana si jambo lisilofaa kwenu; maana, ni maisha yenu, na kwa jambo hili mtazifanya siku zenu kuwa nyingi juu ya nchi….." 32:45, 47

Musa alieleza kwamba baada ya yale mawe mawili ya Amri kuvunjika, Mungu alimwambia achonge mengine, kisha akaenda tena mlima wa Mungu, Sinai, na Mungu akaandika tena zile Amri kumi. Yaonekana Musa alifunga siku 40 zaidi ya mara moja, na kutokunywa maji ukiwa ni mwujiza toka kwa Mungu. Musa akasema watakapotaka mfalme, na Mungu akikubali, basi huyo mfalme azisome na kuzitafakari Sheria za Mungu siku zote za maisha yake ili awe karibu na Mungu. Akasema mfalme asifikiri kuwa yupo juu ya Sheria za Mungu, bali awe mfano wa kutunza Sheria.

Pale ng'ambo ya Yordani iliwekwa miji sita ya kukimbilia kwa yule amwuaye mtu pasipo kukusudia. Mfano katika shughuli za kazi akaangusha mti au kumgonga mtu bila kukusudia. Mtu alikaa pale akingoja kesi ili wajue kweli ni bahati mbaya au alipanga kufanya hivyo. Kama ni bahati mbaya alikaa pale ili ndugu wa yule aliyekufa wasimwue. Alikaa katika miji hii ya makimbilio mpaka kuhani mkuu alipokufa. Yeyote aliyemwua mtu aliyekuwa kwenye miji hii naye pia aliuawa.

Hata leo tunapaswa tuzitunze amri hizi kwa kutokwenda kushoto au kulia. Musa akawaamba wazazi wawafundishe watoto wao na wajukuu amri hizi siku zote za maisha yao. "Sikiza Ee Israeli; BWANA, Mungu wetu, BWANA Ndiye mmoja. Nawe mpende BWANA, Mungu wako, kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na Maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katika macho yako. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako." 6:6-9. Shetani anamwandaa mtoto yoyote ambaye haandaliwi kwenda mbinguni kuwa raia wa jehanamu, hata kwa vitu visivyo na madhara kama vile michezo, kwani hivi vinaweza kuchukua wakati muhimu ambao unapaswa kutumiwa kwa kazi za nyumbani, kazi za shule na ibada binafsi. Iwapo kulikuwa na wakati wa kuwasheheni watoto kwa Neno la Mungu, ni sasa. Shetani ameongeza jitihada zake maradufu katika kuwakamata wachanga kwa kuwarushia jumbe na mambo ambayo yamekusudiwa kuwaangamiza. Unapomwona mtoto amejificha kwenye chumba na simu au kompyuta/tablet/kibao, kuna uwezekano mkubwa anatazama mambo ya kutisha kwenye. Ulaghai wa mtandao umekuwa utaalamu wa vijana wengi. Kupitia njia za moyo, hasa macho na masikio, Shetani anawalisha vijana sumu ili kuwafanya raia wake. Njia ya ufanisi zaidi ya kuwazuia watoto wetu wasianguke kwa mpango wa Shetani ni kuwafundisha Neno la Mungu. Mtoto ambaye akili yake inalishwa na Neno la Mungu kila siku anapewa mtazamo wa ulimwengu wa mbinguni, na kwa neema ya Mungu hataiacha njia. Uwezo ule wa uumbaji ambao ulitamka na malimwengu yakawepo, uko katika Neno la Mungu. Neno hili hutia nguvu; huzaa

maisha. Kila amri ya Mungu ni ahadi; kukubaliwa na mapenzi, kupokelewa ndani ya nafsi, kunaleta pamoja nayo maisha ya Asiye na mwisho. Inabadilisha asili na kuumba upya nafsi katika sura ya Mungu. Wazazi ambao hawana ibada ya kila siku na watoto wao wanampa Shetani uhuru wa nafasi ya kuwalisha na vitu vyake, na Shetani anajitayarisha kwenda kuzimu mtoto yeyote ambaye hajatayarishwa kwenda mbinguni!

Hata leo watu wazima pia wanaamriwa wasimsahau Mungu aliyewatoa katika utumwa wa dhambi bali wamche na kumtumikia, bila kufuata miungu ya watu wengine. Mara nyingi tukiwa na mafanikio na kujenga nyumba nzuri na kukaa na mali au makundi ya ngombe au dhahabu na fedha zinapoongezeka tunasahau kuwa Mungu Ndiye kiongozi wetu. Hata leo Mungu "ameweka mbele yetu baraka au laana, baraka tutakaposikiliza Maagizo Yake atuagizayo na laana ikiwa hatusikiliza Maagizo Yake.

Walikumbushwa kutoacha kutoa sadaka na zaka ya fungu la kumi katika maongezeko yote ya mapato yao ya mashambani, na shughuli zao. Wakakumbushwa kutokuwa na ulaghai wa aina yote kama vile kuondoa mipaka ya jirani.
"Itakuwa utakaposikia sauti ya BWANA Mungu wako kwa bidii, kutunza kuyafanya Maagizo Yake yote nikuagizayo leo, ndipo BWANA Mungu wako, atakapokutukuza juu ya mataifa yote duniani, na baraka zote zitakujia. Utabarikiwa mjini na mashambani na uzao wa tumbo lako au mifugo yako yatabarikiwa. Kapu lako au chombo cha kukandia unga kitabarikiwa. BWANA atawafanya duni maadui zako wakija mbele zako, watakuja kwa njia moja na kukimbia na njia saba." Watakuwa taifa takatifu na mataifa yote watakuwa na hofu kwao. Bwana atawafunulia hazina na watapata mvua kwa wakati. Watakopesha mataifa mengi bali wao hawatakopa. Watakuwa kichwa na wala si mkia, watakuwa juu na wala si chini.

Lakini kama wasiposikia, laana nyingi zitawapata. Watapigwa na maafa na tauni kwa magonjwa mengi kama kifua kikuu, homa, kuwashwa na koga. Hawatapata mvua bali vumbi, adui atawapiga nao watakimbia kwa njia saba. Siku zote wataonewa na kutekwa nyara bila kuokoka. Wataposa mwanamke bali mtu mwingine atamchukua, watajenga nyumba bali mwingine atakaa, watalima matunda bali mwingine atakula mbele ya macho yao, watanyang'anywa wanyama wao na wasirudishiwe. Watoto wao watachukuliwa utumwani na macho yao yataangalia na kuzimia kwa kukosa uwezo wa kufanya lolote. Watakuwa watu wa kushangaza watu, mithali na dharau kati ya mataifa yote. Mgeni aliye kwao atazidi kupanda na wao kushuka, watakopeshwa bali hawataweza kumkopa mtu, kwani watakuwa mkia tu na si kichwa. Kama hawatamtumikia Bwana Mungu kwa furaha na moyo wa kushukuru kwa mema anayowapa, haya yote yatawapata. Kwa nini Mungu alimruhusu wapitie mateso mengi sana? Watakuwa wahitaji, uchi na wenye kiu ya kila kitu. Watakula hata watoto wao, "wanawe aliozaa atawala kwa siri, kwa uhitaji wa vitu vyote." Hakika mawazo ya Mungu ni ya juu sana kuliko yetu na Yeye hufanya yale yanayofaa kwa pande zote mbili. Siku moja tutaambiwa sababu ya haya yote!

Basi haya yakawa Maneno ya agano BWANA alilomwamuru Musa alifanye na wana wa Israeli ngambo ya mto Yordani na akarudia Agano alilolifanya la Amri

Zake chini ya mlima wa Sinai. Musa akasisitiza kuwaambia watu kuwa yale mambo ya siri ni ya BWANA, Mungu lakini mambo yaliyofunuliwa kwao ni ya kwao na watoto wao, ili tuyafanye Maneno yote ya Sheria hii.

Mpendwa mtoto basi ni muhimu kutafakari Maagizo ya BWANA na kuyafanya. Maagizo haya si mazito mno kwetu wala si mbali, si mbinguni hata tuseme tutapandaje kule wala si ngambo ya pili ya bara hata tuseme tutafikaje?

Musa akasema, "Leo nina miaka 120 siwezi tena kutoka na kuingia na BWANA ameniambia hutavuka Yordani. BWANA Mungu wako, Ndiye atakayevuka mbele yako, atawaangamiza mataifa yote nawe utamiliki." Akamwambia Yoshua awe na ushujaa na moyo mkuu, kwani Mungu hatamwacha.

Musa alipomaliza kuandika Sheria na yale aliyowaambia, aliwakabidhi walawi akawaambia waweke chuo kile cha torati kwenye hifadhi ya kando kwenye lile sanduku la Agano, Kumbu 31:26 (Sheria za Musa ni takribani 613, nazo zinahusu mahusiano kwenye jumuiya au taa za trafiki za barabarani). Musa akapanda mlima Nebo, akiwa mwenyewe, mlima wa futi kama 11,900 hivi, inachukua masaa 4 mpaka 9 kupanda. Alikuwa mwenye nguvu zake. Unaweza ukawapa watoto wako zawadi na kuwatendea mema mengi, ila kuwaombea ndiyo jambo kubwa. Musa alikuwa amefanya kazi ya maombezi kwa Israeli kwa miaka mingi! Na hata leo, akiwa kati ya wale wachache walioishi duniani na kuwa mbinguni kama Henoka, na Eliya, kazi yake ya uandishi na maombi yake yanaendelea kutubariki.

*Ni lazima tuombe daima, kwa akili ya unyenyekevu na roho ya upole na unyenyekevu. Hatuhitaji kusubiri nafasi ya kupiga magoti mbele ya MUNGU. Tunaweza kuomba na kuongea na Bwana popote tulipo.


---

Kwa nini Musa alikuwa karibu na Mungu? Alionaje alipokatazwa kwenda nchi ya ahadi? Kwa nini ni vibaya kuwa na miungu mingine? Miungu mingine ni kama nini? Orodhesha baraka na laana za Kumbukumbu la Torati 28.

**SIKU YA 53**
**(Februari 22)**

# Wimbo na kifo cha Musa

**- Hesabu 27 na Kumbukumbu la Torati 31-34**



Katika historia yote Kristo ameachwa nje ya mlango wa mioyo ya watu Wake. Lakini bado Yeye anawapenda. Anaahidi kanisa la Laodikia kwamba ikiwa watamwacha aingie maishani mwao, basi baada ya ujio Wake wa pili atawafanya wakae kwenye kiti Chake cha enzi pamoja Naye (Ufu. 3:21). Yeye Ndiye mpenzi mkubwa zaidi wa ulimwengu wetu. Anatamani kukaa nasi leo na kutupa zaidi ya baraka za kimwili tu. Anataka tumkaribishe ili atawale ndani ya mioyo yetu na kutawala Naye milele. Wote wamkaribishao, hatimaye watakuwa na amri za Mungu mikononi na vipajini mwa nyuso zao, au watakuwa na mbadala bandia wa shetani ili waweze kununua na kuuza. Changamoto za dunia ni nyingi na siyo rahisi kuwa na umakini, ila hebu liwe lengo letu leo kuwemo miongoni wa waimbaji wa ile kwaya kubwa ya mbinguni! Kwa muhtasari, wimbo wa Musa unasema kwamba Mungu ni mwema; kutomtii kunasababisha maafa. Watakatifu wataimba wimbo wa Musa (Kutoka 15) na ule wa Mwana-Kondoo kwenye bahari ya kioo (Ufunuo 15). Wimbo huu, (Kumbukumbu 32:1-43) unawakumbusha Waisraeli uhusiano wao wa agano lao na Mungu. Takribani, mtu anaweza kuuchambua wimbo huu hivi: Hakika Maandiko yanafaa kwa kuonya na kufundisha. Kitabu hiki chasikitisha ila kinaendelea kutukumbusha kwamba Mungu ni mwingi wa rehema Naye hutusamehe dhambi zetu, ila tutavuna matokeo ya dhambi hizo. Kwa bahati mbaya jamii ya binadamu inaendelea kuishi maisha ya kutotii. Nina hakika Musa akitazama chini kutoka mbinguni anajiuliza jinsi tunavyoweza kuendelea kutenda dhambi baada ya kusoma yote kumhusu yeye na maisha ya wana wa Israeli. Hebu tutambue ubaya wa dhambi na kuanza kutii amri na sheria Zake Mungu, hiyo itatusaidia mahusiano Naye na kuwemo Kanani ya mbinguni. Mungu atusaidie.

BWANA akamwambia Musa apande mlima wa Abarimu na aitazame nchi aliyowapa Waisraeli. Akasema, "nawe ukisha kuiona, wewe nawe utakusanyika pamoja na baba zako kama Haruni ndugu yako alivyokusanyika.' Akamkumbusha kwamba

kuasi kwake na nduguye katika jangwa la Sini wakati wa mateto ya mkutano kumemfanya abaki ngambo, "wala hamkunistahi, hapo majini mbele ya macho yao". Maji haya yalikuwa maji ya Meriba. Musa akamwomba BWANA aweke mtu atakayetoka mbele ya mkutano na kuingia mbele yao ili wasiwe kama kondoo wasio na mchungaji. Ndipo BWANA akamwambia amchukue Yoshua na kumwekea mikono "mtu mwenye roho ndani yake". Akaambiwa ampe mausia mbele ya kuhani Eleazari na watu. Na akamwambia Musa aweke juu yake sehemu ya "heshima yake." Naye Yoshua angesimama mbele ya Eleazari kuhani naye atamwulizia hukumu mbele za Bwana. Kwa Neno Lake watatoka, na kwa Neno Lake wataingia, yeye na wana wa Israeli wote pamoja naye na mkutano pia. Musa akafanya kama Mungu alivyoagiza.

Hata leo Mungu ametuwekea viongozi, hebu tuepuke kuwapa majaribu ya kufanya dhambi, kwa manunguniko yetu na kukataa kutii yale wanayotuongoza ambayo BWANA anataka tuyafanye. Wazazi wetu pia ni viongozi ambao Mungu ametuwekea tuwatii, tusiwahuzunishe na kuwafanya watende dhambi kwa ukaidi wetu au kutaka kutenda vitendo viovu. Musa alikuwa kiongozi shujaa, hata alimwomba Mungu akisema, "Nionyeshe njia Zako BWANA kama nimepata kibali machoni pako ili nitembee katika hizo ili nikutumikie vyema na kupata kibali machoni pako". Mungu alimwakikishia Musa kwamba "uso Wangu utakwenda pamoja nawe, Nami nitakupa raha.....umepata neema machoni Pangu, Nami nakujua jina lako". Maneno matamu hakika! Hata leo Mungu anakujua jina lako, je, unapenda kujua njia Zake? Basi Yeye Yupo tayari kukufadhili na kukurehemu.

Musa alikuwa amewaambia kuwa kwa vile Mungu aliwapenda angewafanyia mambo makubwa, ila aliwakumbusha kwamba inabidi watii Amri Zake na kwenda katika njia Zake ndipo watapata baraka hizi. Wangebarikiwa watokapo na waingiapo, wangebarikiwa mashambani na nyumbani na hata nje ya nchi yao. Mungu angefungua hazina Zake kwao na "wangekuwa vichwa na wala si mkia". Akasisitiza kwamba wakae karibu na Mungu na kutenda Mapenzi Yake. Akawaambia kile kitakachotokea kama wakiasi Amri Zake.

Musa akapanda uwanda wa Moabu mpaka mlima Nebo, kilele cha Pisga kukabili Yeriko. Mungu akamwonesha nchi yote ambayo makabila ya Israeli walikuwa wanakwenda kuingia. Bwana akamwonesha nchi yote na kumwambia, "Hii ndiyo nchi Niliyomwapia, Ibrahimu, na Isaka na Yakobo, nikisema nitawapa wazao wako. Basi nimekuonyesha kwa macho yako, lakini hutavuka huko." Musa alipewa kuona kusiko kwa kibinadamu, ilikuwa kama sinema akaona mashariki, magharibi, kusini na kaskazini. Akaona wana wa Israeli wanachukua nchi, mpaka wanaanza maisha mapya. Hakika Mungu alimpenda Musa.

Baada ya wosia, Musa alipanda mlimani peke yake. Basi Musa, mtumishi wa Mungu akafa huko katika nchi ya Moabu. Musa alikuwa mtu wa miaka 120 alipokufa akiwa kama kijana tu! Jicho Lake halikupofuka wala nguvu za mwili Wake hazikupunguka. Haruni alipokuwa anataka kulala na baba zake alipanda na Musa na Huri, bali Musa alipanda peke yake mlima Pisga. Akatazama kambi chini, na kuona nchi nzuri waliyopewa. Kisha akalala. Wana wa Israeli wakamwomboleza Musa kwa siku

thelathini. Musa alisihi aende kwenye "nchi ile nzuri!"—lakini Mungu akasema L!. Loo, lakini Mungu alimwonyesha Musa, kutoka kilele cha Mlima Nebo, Nchi ya Ahadi—yote hayo—katika uzuri wa majira ya kuchipua! Kisha Musa akalala chini, na akafa, na Mungu akamzika. Je, Yesu alingoja muda gani kabla ya kurudi kwa Musa? Yuda anadokeza kwamba Shetani alitaka kumweka Musa katika kaburi hilo, na kumshindilia humo! Lakini Yesu hakubishana naye na hivyo alimfufua Musa. (Shetani anaweza kufikiria kuwa ndiye anayeongoza, lakini sivyo!). Karne 14 baadaye Yesu alipokuja duniani kama mmoja wetu, kabla tu hajatoa dhabihu ya mwili wake kwa ajili ya wokovu wetu, Musa—pamoja na Eliya—walishuka kutoka mbinguni ili kumtia moyo Yesu kwenye Mlima wa Kugeuzwa Sura kwa mng'ao. Alipata kusimama katika Nchi ya Ahadi hatimaye baada ya hayo yote!

Naye Yoshua mwana wa Nuni akiwa amejaa roho ya hekima akachukua nafasi ya Musa. Katika kitabu cha Yuda, tunaona miujiza ya ajabu. Mungu alimfufua Musa na kumchukua mbinguni. Shetani aligombania mwili wa Musa akimshtaki Musa kwamba alifanya dhambi, bali Mungu alikuwa ameona toba ya Musa, uvumilivu na mateso aliyopata, na kumchukua. Biblia inasema mpaka hivi leo watu hawajui kaburi la Musa. Pengine wangeabudu kaburi!

Tunaambiwa kuwa mbinguni tutaimba wimbo wa Musa na wa Mwana-Kondoo, hakika Musa alikuwa mtumishi wa Mungu aliye karibu Naye. Wewe na mimi sasa ni sehemu ya watu wa kiroho wa Israeli na Kristo anakuja upesi kutupeleka kwenye nchi ya ahadi. Ni matukio gani unakumbuka zaidi katika maisha yako? Je, unaweza kueleza maajabu na miujiza ambayo Mungu alikufanyia katika safari ya maisha? Je, unaweza kutathmini nyakati ambazo ulimwasi Mungu na jinsi Mungu alivyotenda? Waambie watu wengine kile ambacho Mungu alichokufanyia na kupitia wewe ulipokuwa njiani kuelekea ufalme wa Mungu. Kumbuka, Mungu ni Mwaminifu. ujiweke zaidi kwa Yesu ili atutumie kuwaokoa wanaoangamia. Kutoka kwa Waisraeli Misri kulikuwa ni mfano wa msafara wa watoto wa Mungu kutoka katika ulimwengu huu wa dhambi na ole ni mfano, na uko karibu!

Twafikiri kuwa Roho Mtakatifu alimwongoza Yoshua kuandika mistari ya kumalizia Kumbukumbu la Torati. Musa ametuonyesha kile tunachopaswa kufanya wakati kufa kwetu kunapofika. Twapaswa kuangalia maisha yetu ya nyuma na kuungama dhambi zote tunazoweza kukumbuka. Kama vile Musa alivyohakikishiwa msamaha, vivyo hivyo mwizi msalabani alipewa uhakikisho wa msamaha. Kwa hiyo watu hawa wawili walikuwa na uhakika wa wokovu wao walipokuwa wanakufa. Hakuna Mkristo anayepaswa kufa bila uhakikisho wa wokovu, wakati Yesu amesimama Patakatifu pa mbinguni, akituhudumia (Ebr 4:14-16). Lakini kungoja au kuchelewa hadi dakika ya mwisho kuungama au kutubu dhambi zetu kunaweza kuwa hatari. Hii ni kwa sababu kifo kinaweza kuja ghafla kupitia ajali au magonjwa. Hivyo Leo, tutakapoisikia sauti Yake, Tusiifanye migumu mioyo yetu kuwa migumu kwa uasi. Unaweza kujifunza mengi kutoka kwa maneno ya mwisho na matendo ya mwisho anayejua anakwenda kufa. Musa ametushirikisha maneno yake ya mwisho na sasa tunaona matendo yake ya mwisho: analitii Neno la BWANA. Ninakumbushwa Maneno na matendo ya mwisho ya Yesu: "Baba, si mapenzi Yangu, bali Yako yatimizwe. Baba mikononi Mwako naiweka Roho Yangu. Huu ndiyo mfano wa

kufuata! Kujisalimisha mkamilifu kwa utii wenye upendo. Hayo ndiyo maombi yangu kwa maisha yangu leo. Na wewe je? Musa alikuwa na amani kwa sababu akili yake ilikuwa imekaa kwa Mungu. Sijui ni muda gani ulipita toka alipokufa mpaka alipofufuliwa, lakini ningependa kufikiri kwamba haikuwa muda mrefu hivyo. Bwana alitamani kuendelea mahusiano na rafiki Yake wa karibu! Musa Alipoona kupaa kwa Mwokozi na kuona kwamba Yeye Mwenyewe angekuwa mmoja wa wale wanaopaswa kumkaribisha Mwokozi na kumfungulia milango ya milele, ni tabasamu la namna gani lililotokea usoni mwake! Hakuna lugha inayoweza kuelezea furaha, utukufu, na nuru iliyong'aa kutoka usoni mwake. Hakuna kalamu inayoweza kuchora hiyo picha au Kamera inayoweza kuchukua taswira. Ni ufunuo wa ajabu kiasi gani!

Mungu anatamani kutupa uzima bure leo. Hebu tuwe waaminifu ili tuwepo katika zile enzi zisizo na kikomo za umilele pamoja na Rafiki na Mwokozi wetu. Tumeona Mungu Mwenyewe alimzika Musa. Ni upendeleo ulioje kuzikwa na Mungu Mwenyewe! Musa alifufuliwa kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Yuda. Yeye ni mfano wa wale ambao watakufa katika Kristo na kupata kufufuka siku parapanda ya mwisho. Mungu anajua mahali ambapo kila mmoja wa watoto Wake amezikwa leo, na historia ya dunia itakapofungwa atawaita wote kutoka makaburini na sote tutasema "Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako? Uchungu wa mauti ni dhambi, na nguvu za dhambi ni torati. Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo" Shetani anataka sisi sote tuwe wafu milele, lakini Kristo alikuja kuturudishia uzima kama ulivyotolewa awali kwa Adamu na Hawa kabla hawajatenda dhambi na uzima tele zaidi ya huo, kwani dhambi haitainua kichwa tena, milele zote!

*Maombi ya Hadharani yanapaswa Kuwa mafupi nayo yaambatane na Sauti ya asili—Baadhi ya Maombi marefu yanayotolewa na wahudumu yamekuwa yasiyo na mafanikio (yamefeli). Kuomba sala refu kama wengine wanavyofanya sio sawa, kwani sio mahali pake. Wanaumiza koo na viungo vya sauti, na kisha wanazungumza juu ya kuvunjika afya kwa kazi yao ngumu. Wanajiumiza wenyewe wakati haipaswi kuwa hivyo. Wengi huhisi kwamba kusali huumiza viungo vyao vya sauti zaidi kuliko kuzungumza. Hili ni tunda la kuweka mwili kwa mkao usio wa kawaida, na jinsi ya kichwa kinavyowekwa. Wanaweza kusimama na kuzungumza, na wasijisikie kujeruhiwa. Mkao wa maombi (position) unapaswa kuwa ya asili kabisa. Kuomba kwa muda mrefu kunachosha, na si kwa mujibu wa injili ya Kristo. Nusu au hata robo ya saa ni ndefu sana. Muda wa dakika chache unatosha kuleta haja zako mbele za MUNGU na kumwambia kile unachotaka; na unaweza kuwachukua watu pamoja nawe na bado usiwachoshe na kupunguza hamu yao katika ibada na sala. Wanaweza kuburudishwa na kuimarishwa, badala ya kuchoka.

---

Kwa nini Musa anaelezewa kwamba alikuwa na imani? Kwa nini Shetani aligombana na Mungu? Je, Maandiko yanasemaje kwa wale waliokufa? Je, Mungu ameahidi uzima wa milele kwa waovu? Jina jingine la mlima Nebo ni nini? Taja baraka na laana za Kumbukumbu la Torati 28. Dhambi ya Musa ilikuwa nini?

**SIKU YA 54**
**(Februari 23)**

# Rahabu na Kamba Nyekundu

**- Yoshua 1-3**

Baada ya kufa kwa Musa, Mungu alimtokea Yoshua na kumwambia, "Musa mtumishi Wangu amekufa; haya, basi, ondoka, vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote ...". Yoshua akachukua uongozi, Bwana akamwambia mipaka ya nchi ya Kanaani. Kisha akamwambia "kama nilivyokuwa pamoja na Musa ndiyo nitakavyokuwa pamoja na wewe, sitakupungukia wala sitakuacha, uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa nchi hii." Akarudia kumwambia, "uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie na kutenda sawasawa na Sheria yote aliyokuamuru Musa...usiiache, kwenda mkono wa kuume au wa kushoto, upate kufanikiwa sana kila uendako. Kitabu cha torati kisiondoke kinywani mwako bali yatafakari Maneno Yake mchana na usiku upate kuangalia kutenda sawasawa na Maneno yote yaliyoandikwa humo. Je! Si Mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa usiogope wala usifadhaike kwa kuwa BWANA, Mungu wako, Yu pamoja nawe kila uendako." Vitabu vingi vimeandikwa juu ya uongozi, lakini kitabu bora kuliko vyote ni kile ambacho Mungu Mwenyewe alimwambia Yoshua cha kufanya, yaani Biblia. Viongozi walio na nguvu na ujasiri katika kutumia kanuni za Biblia kwa vitendo kwenye utawala hufaulu, ingawa siyo maarufu au wanaweza wasipendwe. Haruni alipendwa, lakini alishindwa vibaya kwa sababu, alikuwa hana msimamo, alikubali matakwa ya watu na kuwatengenezea ndama wa dhahabu. Mtu fulani amesema, "Ikiwa unataka kumfurahisha kila mtu, usiwe kiongozi bali uza 'ice cream/barafu'. Kiongozi, anahitaji ujasiri na kuondoa vihofu, huku akiwa mtiifu kabisa kwa Kristo. Chakula chake, mavazi, mtindo wa uongozi, mwenendo, vyapaswa vimwakilishe Bwana. Kiongozi yoyote yule anapaswa kusoma Yoshua 1:7-9 anapokuwa na msongo.

Naye Yoshua akaanza kazi kwa kutuma watu wawili kwa siri kuipeleleza Yeriko. Wakaenda na kufika nyumba ya kahaba mmoja aitwaye Rahabu akawakaribisha na kuwatendea kwa ukarimu. Mfalme wa Yeriko akaambiwa kuwa wapelelezi wamo kwenye nchi yao. Mfalme akatuma watu, bila shaka wanajeshi, wakapiga hodi kwa Rahabu na kuamrisha, "watoe watu wale waliokuja kwako maana wamekuja kuipeleleza nchi." Rahabu aliwaficha darini wale wapelelezi kwa mabua ya kitani, na kusema "Naam, wale watu walikuja kwangu lakini sikujua walikotoka..... wafuateni upesi maana mtawapata." Akijua kwamba wanajeshi wameshaenda mbele tayari aliwatoa wale wapelelezi kwenye mabua na kuwaambia, "Mimi najua ya kuwa BWANA amewapa ninyi nchi hii, na ya kuwa hofu imetuangukia mbele yenu, na kuwa wenyeji wote wa nchi wanayeyuka mbele yenu. Maana tumesikia jinsi BWANA alivyokausha maji ya bahari ya Shamu mbele yenu, hapo mlipotoka Misri, tena mambo hayo mliyowatendea wafalme wawili wa Waamori waliokuwa ngambo ya mto Yordani, Sihoni na Ogu, mliowaangamiza kabisa. Na mara tuliposikia mioyo yetu iliyeyuka wala haukusalia ujasiri wo wote katika mtu awaye yote, kwa sababu

yenu, kwa kuwa Mungu wenu, Yeye Ndiye Mungu, katika mbingu juu na katika nchi chini. Basi sasa nawasihi, niapieni kwa BWANA, kwa kuwa nimewatendea hisani, ninyi nanyi mtaitendea hisani nyumba ya baba yangu; tena nipeni alama ya uaminifu ya kwamba mtawaponya hai baba yangu na mama yangu, na ndugu zangu wanaume na wanawake, na vitu vyote walivyonavyo na kutuokoa roho zetu na kufa." Wale wanaume wapelelezi wakamhakikishia kwamba, "uhai wetu badala ya uhai wenu, ikiwa hamtangazi habari ya shughuli hii … BWANA atakapotupa nchi hii, tutakutendea kwa hisani na uaminifu. Basi Rahabu akawashusha wale watu wawili kwa kamba dirishani, maana nyumba yake ilikuwa katika ukuta wa mji, naye alikaa ukutani." Akawaambia waende mlimani wale wanaowafuatia wasije wakawapata na wajifiche kule siku tatu hata hao wanaowatafuta watakaporudi, "kisha nendeni zenu". Wale wapelelezi wakamwambia Rahabu hawataki hatia kwa ajili ya kiapo walichokula hivyo Rahabu afunge "kamba hii nyekundu" katika dirisha alilowatelemshia, kisha akusanye jamaa zake na ndugu zake wote na itakuwa mtu awaye yote atakayetoka katika mlango wa nyumba yake na kwenda njiani damu yake itakuwa juu ya kichwa chake mwenyewe nao watakuwa hawana hatia. Ila mtu ambaye atakuwa ndani ya nyumba yake damu yake itakuwa na hatia juu yao wapelelezi. Basi Rahabu akakubaliana nao na kuwatoa wapelelezi, nao wakaenda zao. Akaifunga ile kamba nyekundu dirishani na wakafuata Maagizo Yake ya kwenda milimani na kujificha siku tatu. Kisha wakatelemka mlimani na kumwendea Yoshua kumpa tarifa, "BWANA ameitia nchi yote katika mikono yetu, tena kuzidi ya hao wenyeji wa nchi wanayeyuka mbele yetu."

Japo Rahabu hakumjua Mungu wa mbinguni vizuri, aliokolewa kwa kuwasaidia watu wa Mungu na hatimaye kuwa mfuasi wa Mwenyezi, ndio maana katika Waebrania 11:31 tunasoma, "Kwa imani Rahabu yule kahaba hakuangamia pamoja na hao walioasi, kwa kuwa aliwakaribishsa wale wapelelezi kwa imani." Kuwa mkarimu kwa watu wenye mahitaji au wageni ni jambo muhimu. "Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa Jina Lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu, na hata sasa hivi mngali mkifanya vile. Na tunataka kila mmoja wenu aonyeshe bidii iyo hiyo kwa utimilifu wa tumaini hata mwisho, ili msiwe wavivu, bali muige wale wazirithio ahadi kwa imani na subira. Kahaba asiye Myahudi, ambaye hakuona miujiza hii yote lakini alisikia habari zake akaziamini na kuokolewa. Watu ndani ya kanisa wanaweza kupotea, wakati watu wa tabia mbovu, ambao kwa sasa wako nje ya kanisa, wanaweza hatimaye kuwa waumini na kuokolewa. Kwa hiyo, usimkatie tamaa mtu yeyote, kwa muda mrefu wakati kuna pumzi mwilini bado, kuna matumaini.

Zaidi ya hayo, ni wazi kwamba vikundi vyote vya watu Waisraeli waliamriwa kuwaangamiza kabisa wale watu wa mataifa ambao kikombe chao cha ghadhabu kilikuwa kimefurika, nao hawakufanya vile. Watu hao wanajitokeza baadaye katika Maandiko. Kwa mfano, Rahabu na familia yake yote waliokolewa kutokana na uharibifu wa Yeriko (Yoshua 2). Hata alifanikiwa kuingia katika "Ukumbi wa Imani" wa Waebrania 11. Fikiria pia wengine wasio Waisraeli ambao wamekaribishwa katika taifa la Israeli: watu kama Yethro Mmidiani na Ruthu Mmoabu, Wagibeoni, Uria Mhiti, Wamisri katika kundi mseto kutoka Misri, kwa kutaja mifano michache. Rahabu ametajwa tena katika injili kwenye mbari ya Yesu. Yeye alikuwa bibi au

nyanya wa mfalme Daudi baadaye, kwani aliolewa na Salmoni, na kuzaa mtoto aitwaye Boazi, na Boazi akamzaa Yese na Yese akamzaa mfalme Daudi na mfalme Daudi akamzaa mfalme Sulemani! Kisa cha ajabu.

*Makosa yamefanywa na wengi katika mazoezi yao ya kidini katika kuomba kwa muda mrefu na kuhubiri kwa muda mrefu, kwa kupayuka au kutumia sauti ya juu sana, kwa sauti ya kulazimisha, kwa mkazo usio wa asili na sauti isiyo ya asili.

---

Baada ya Musa kufa, Mungu alimwambiaje Yoshua? Rahabu aliwaambiaje wale wapelelezi? Wapelelezi walileta taarifa gani kwa watu? Kwa nini Rahabu anatajwa kama mwenye imani? Boazi ni nani? Kwa nini Mungu alimwagiza Yoshua asisahau kusoma Torati, na aitafakari mchana na usiku?

**SIKU YA 55**
**(Februari 24)**

# Kuvuka Mto Yordani

**- Yoshua 3-5**



Basi wakatoka Shitimu ngambo ya mto Yordani na Yoshua na wana wa Israeli wakakaa hapo kabla ya kuvuka. Mto huu ulikuwa unafurika, na ulikuwa na mkondo mkali na kina. Waisraeli hawakuwa na boti, mashua wala meli. Huenda wengine walijiuliza "tutavukaje na mto huu unafurika?" Ndipo viongozi wakapita na kusema, "mtakapoliona Sanduku la Agano la BWANA Mungu wenu na makuhani Walawi wakilichukua ndipo mtakapoondoka hapa mlipo na kulifuata." Ila msilikaribie. Yoshua akawaambia wajitakase maana BWANA atatenda mambo ya ajabu kati yao. Basi Yoshua akawaambia makuhani waliinue sanduku la agano na wavuke mbele ya hao watu. BWANA akamwambia Yoshua, "Hivi leo Nitaanza kukutukuza mbele ya Israeli wote, wapate kujua ya kuwa Mimi nitakuwa pamoja na wewe kama nilivyokuwa na Musa." Akaamuru awaambie makuhani wakifika kwenye maji ya mto Yordani wasimame. Yoshua akawaambia watu waje kusikia ili wajue Mungu Aliye hai yu kati yao na kuwa hatakosa kuwafukuza mbele yao Mkaanani, Mhiti, Mhivi, Myebusi, Mperizi, Mgirgashi, na Mwamori.

Yoshua akasema itakuwa wakati nyayo za makuhani waliochukua sanduku la BWANA, BWANA wa dunia yote, zitakaposimama katika maji ya Yordani, hayo maji ya Yordani yatatindika, maji yale yashukayo kutoka juu nayo yatasimama kama kichuguu au ukuta. Basi walitoka katika hema zao ili kuvuka Yordani. Makuhani walilichukua sanduku la agano wakitangulia mbele ya watu; na nyayo zao zilipogusa tu maji ya ukingoni (maana Yordani hujaa hata kingo zake zikafurika wakati wa mavuno) maji yakainuka na kusimama kama fungu au kichuguu hivi. Maji yakakoma kabisa na makuhani waliolichukua sanduku la BWANA wakasimama imara mahali pakavu kabisa na taifa lote la Israeli wakavuka tena katika nchi kavu. Walipomaliza kuvuka, BWANA akanena na Yoshua kuwa atwae watu kumi na wawili. Kila mmoja akiwakilisha kabila la Israeli, watu hao watwae mawe kumi na mawili hapo katikati ya Yordani, mahali hapo miguu ya makuhani iliposimama imara, waende na hayo mawe na kuyaweka kambini watakapolala usiku.

Basi Joshua akawatayarisha hawa watu 12 na kumwambia kila mtu abebe jiwe begani ili kwamba jambo hili liwe ishara au kumbukumbu kwa vizazi vijavyo ambavyo havikuona haya, watakapouliza. Kila jiwe lililiwakisha kabila. Ushuhuda wa matendo makuu ya BWANA ni muhimu, ni jambo jema kumsifu BWANA na kuliimbia Jina Lake. Watoto, wajukuu na vitukuu watakapouliza wakiona yale mawe wajibiwe kwamba, "Maji ya Yordani yalitindika kabisa mbele ya sanduku la BWANA." Waliyapata mawe katikati ya Yordani kirahisi kwa sababu ya mkono wa BWANA. Hii ilikuwa mara ya pili kuvushwa kwenye maji ya kina, mara ya kwanza ikiwa maji ya Bahari ya Shamu, na sasa maji ya mto Yordani. Yoshua akapanga yale mawe kumi na mawili ukingoni mwa ya Yordani, mahali pale miguu ya hao makuhani walolichukua hilo sanduku iliposimama, na Neno la Mungu likiandikwa, bado mawe haya yalikuwepo. Yordani iligawanyika sehemu mbili ili nao watembee nchi kavu. Huenda tusiweke mawe ili kukumbuka baraka ambazo tumezipokea kutoka kwa Mungu, lakini tunaweza kuziandika katika shajara, na kwa kusoma mara kwa mara kutaifanya imani yetu iwe hai na yenye nguvu. Mahali hapa paliitwa Gilgali. Makuhani walivuka haraka baada ya watu wote kuvuka, na kuchukua mawe na kuyapanga kwenye lundo. Waliangalia tena mto wakaona maji yamekuja tena na kujaa. Hakika BWANA anatenda maajabu hata siku za leo nami siwezi kuelezea yote. Hatuna haja ya kuogopa mambo ya siku zijazo, isipokuwa tu tutasahau njia ambayo Bwana ametuongoza, na mafundisho Yake katika historia yetu iliyopita. Mungu ni Yule Yule jana, leo na hata milele. Ikiwa tutakumbuka miujiza Aliyoifanya kwetu katika siku zilizopita, hatutakuwa na hofu kwa changamoto yoyote tunayoikabili leo, au kesho. Sote tumeitwa kuacha urithi unaomwonyesha Mungu kwenye vizazi vijavyo. Ushuhuda wetu ni ushahidi kwa wale wanaofuata. Je, wewe leo unaacha urithi gani?

Wana wa Reubeni, Gadi, na nusu ya manase walivuka hali wamevaa silaha mbele ya wana wa Israeli, wakiwa tayari na silaha kwa vita. Makabila haya waliomba wapewe urithi karibu na mto wa Yordani wenye rutuba upande ule kabla ya kuvuka. Walipomwambia Kiongozi, alisikitika kuwa hawataki kusaidia ndugu zao kukomboa nchi. Hata hivyo walihahidi kwenda kuwasaidia ndugu zao kukomboa Kanaani nzima, kisha warudi ng'ambo ya Yordani tena ili kuishi na kumiliki nchi. Wake zao na watoto walibaki, bali wanaume hawa walienda vitani. Basi siku hii

Bwana alimtukuza Yoshua mbele ya macho ya Israeli wote, nao wakamheshimu jinsi walivyomheshimu Musa.

Waamori waliposikia jinsi Bwana alivyokausha maji ya Yordani mbele ya Waisraeli hata wakavuka, mioyo yao ikayeyuka kwa hofu, wala haikuwamo roho ya nguvu ndani yao tena, kwa ajili ya wana wa Israeli. Maisha ni vita. Wote wanaotaka Mungu awapiganie vita vyao lazima wajifunze kumtii Mungu kabisa. Wanapaswa kumtumaini Bwana kwa mioyo yao yote, na wasitegemee akili zao wenyewe (Mithali 3:5). Basi kutakuwa na ushindi kama Waisraeli huko Yeriko.

Leo nasi tuondoke kwa imani na tumruhusu Mungu atufanyie mambo ya ajabu "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni." Mt. 5:16. Tujiweke wakfu (kutahiriwa kwa moyo).
Tumruhusu Roho afanye kazi ndani yetu binafsi. Tuvue viatu vyetu pale kwenye uwepo wa Mungu. Tusiogope maadui kwa sababu Mungu anaahidi hivi: "Nitapeleka hofu Yangu mbele yako, Nami nitaleta machafuko kati ya watu wote utakaowajia, Nami nitawafanya adui zako wote wakupe visogo." Kutoka 23:27. "Ikiwa Mungu yuko upande wetu, ni nani aliye juu yetu?" Warumi 8:3

*Zungumza kwa Uwazi na toa sala kwa Uwazi—Kwa kielelezo chako mwenyewe wafundishe watoto wako kusali kwa sauti iliyo wazi na iliyo tofauti. Wafundishe kuinua vichwa vyao kutoka kwenye kiti na kamwe wasifunike nyuso zao kwa mikono yao. Kwa kufanya hivyo wanaweza kutoa maombi yao sahili, wakirudia sala ya Bwana kwa pamoja.

---

Je, Waisraeli walivukaje mto Yordani? Nani walitangulia? Bwana alimtukuzaje Yoshua siku hiyo? Mawe ya Gilgali yalitoka wapi? Kwa nini mioyo ya Waamori iliyeyuka? Je, unakumbuka mwujiza wowote Bwana aliokutendea au kuwatendea wazazi wako? Muujiza wa kuvuka kwenye Maji mengi ulitendeka wapi tena, mbali na Yordani

**SIKU YA 56**
**(Februari 25)**

# Yoshua Akutana na Kamanda wa Majeshi

**- Yoshua 5 na 6**



Miguu yao sasa ilikuwa imekanyaga Kanaani, ile nchi ya ahadi, wakamshukuru Mungu kwa kuwakomboa toka utumwani na hata kuwavusha mto Yordani. Nasi leo pia Mungu anatuvusha katika matatizo mbali mbali. Yoshua akaagizwa wanaume wote watahiriwe kwa vile walizaliwa na kusafiri jangwani bila tohara. Tohara wakati ule ilikuwa ni agano kati yao na Mungu. Wana wa Israeli wakaadhimisha Pasaka, nao wakaanza kulima na kupata mazao ya nchi,wakala mikate na bisi au nafaka za kuoka, na hapo ndipo Mana ikakoma kunyesha tena baada ya kula mazao ya nchi. Mungu wetu Ndiye anatoa mahitaji yetu, hivyo ni vyema kuomba atupatie riziki zetu siku kwa siku.

Ikawa Yoshua alipokuwa karibu na mji wa Yeriko, akijitenga na watu ili kuomba hekima na mipango kwa Bwana, maana alikuwa anakabiliwa na mataifa mengi ambayo ilibidi apigane nayo ili kuimiliki nchi. Aliona ukuta wa Yeriko, na miji mingine mingi yenye majitu katili na wenye uzoefu wa vita ukilinganisha na watu wao waliokuwa utumwani. Mara akatazama na kwa kuangalia vizuri akamwona

Mwanamume akiwa amesimama mbele yake kumkabili na alikuwa na upanga wazi mkononi mwake. Yoshua akamwendea na kumwuliza. “Je! Wewe u upande wetu, au upande wa adui zetu? Yule mtu akajibu, “La!, lakina nimekuja sasa, Mimi ni Amiri wa jeshi la BWANA.” Ndipo alipogundua anazungumza na nani! Alikuwa ni Yule ambaye Ibrahimu alimkaribisha na Yule aliyeshindana na Yakobo mpaka asubuhi. Yoshua akaanguka kifudifudi na kumsujudia. Mara alipogundua Huyu ni BWANA akasema, “BWANA wangu ananiambia nini mimi mtumishi Wake?” Mungu alikuwa ana mipango mingi Kwake ila jambo la kwanza alisema awe na kicho mbele za BWANA. Ndipo BWANA Ambaye ni amiri jeshi wa jeshi la BWANA akamwambia Yoshua vile alivyomwambia Musa “Vua viatu vyako miguuni mwako, kwa kuwa mahali hapa usimamapo ni Patakatifu. Yoshua akafanya hivyo.

Ndipo Bwana akampa mipango ya kuuteka Yeriko. Watu wa Yeriko walikuwa wamefunga milango ya mji wao kabisa kwa sababu ya wana wa Israeli. Walikuwa siku hizo wakikaa kwenye miji yenye ngome au kuta kubwa na mageti makubwa. Walishangaa mbona Waisraeli hawawavamii, maana wao walikuwa wamejiweka tayari kwa vita, iwe ni mavazi au silaha. BWANA akamwambia Yoshua tazama nimeutia Yeriko, yaani mashujaa wake na mfalme katika mikono yake. Akaamuru wazunguke mji ule mara moja kila siku kwa siku sita, kisha siku ya saba wazunguke mara saba, lakini safari sita iwe kimya kimya. Makuhani saba wanaozunguka wachukue tarumbeta saba za pembe za kondoo waume, mbele ya hilo sanduku la Agano. Siku ya saba wakimaliza kuzunguka mara sita, ya saba makuhani wapige tarumbeta zao kwa nguvu, na watu wote wapige kelele kwa sauti kuu, na ukuta wa mji utaanguka chini pale pale, na watu wa upande ukuta huo na kuingia mjini. Yoshua aliwaita makuhani na kuwapa Maagizo kuchukua sanduku la agano na kufanya kama walivyoagizwa.

Bila shaka watu wa Yeriko walishangaa wakajaa ukutani na huenda kujiuliza, “ni nini hiki kinachoendelea hapa, watu wanazunguka tu kimya kimya kila siku?” BWANA alikuwa amewapa mji. Ukuta ulipokuwa chini waliingia mjini na kukabili mbele wakautwaa mji. Wakaangamiza kila kilichokuwa katika mji. Wakaambiwa mji huu na vitu vyake vitakuwa wakfu kwa ajili ya Bwana. Walimwacha Rahabu na watu wake hai kwa sababu aliwaficha wale wapelelezi. Wapelelezi wawili walienda kumtoa Rahabu na vitu vyake na jamaa zake kisha wakauteketeza mji kwa moto. Bali vitu vya shaba, dhahabu au chuma vitaletwa kwenye hazina ya BWANA na kuwa vitakatifu.

BWANA anatatua matatizo yetu, na mambo mazito makubwa huyarahisisha na matata atageuza, yawe kwetu ya baraka. Tusitembee tukilalamika, kusengenya au kupayuka, maana pigano ni la BWANA. Lakini inatupasa tujitoe kikamilifu, wazungu wanasema “Tujisalimishe.” Mtandao umefungua njia mpya kabisa ya kuwasiliana na kushiriki injili unapotumiwa vizuri nao utaweza kuangusha kuta za Yeriko na tukaingia humo ndani. Yatupasa tuombe ushauri kutoka kwa Mungu kwa maombi na kufunga. Kanisa langu hutoa mfundisho siku ya Sabato kwenye Facebook na YouTube, na watu hufuatilia kote ulimwenguni. Huduma nyingine nyingi huleta vipindi vya maswali na majibu, muziki, afya, ushauri nasaha, familia, uinjilisti na malezi. Baadhi ya watu hugundua imani ya Kikristo kupitia yale wanayopata

kwenye mtandao wa redio, runinga na tovuti. Tunahitaji kujifunza matumizi ya zana hizi ili kuufikia ulimwengu pamoja na nyenzo ambazo tumekuwa tukizitumia za kumtembelea mtu mmoja mmoja nyumba kwa nyumba.

Jambo jingine tunaona ni kugawanya kwa nchi kulifanywa na Yoshua na Eleazari, kuhani mkuu huko Shilo mbele za Bwana kwenye lango la Patakatifu ambalo lilikuwa limesimamishwa huko Shilo. Hii ilionyesha kwamba Mmiliki wa asili na halali wa nchi alikuwa ni Bwana Mwenyewe. Hata sisi leo kama tungefuatilia hati za ardhi ambazo sisi tunamiliki binafsi hadi kwa wamiliki wa asili, na kwenda mbele, hatimaye tungefika kwa Mungu. Sisi sio wamiliki halisi: sisi ni wapangaji wa ardhiau wakodishaji, na Bwana siku moja atatuuliza ni kwa jinsi gani tumetumia mali Yake na kwa madhumuni gani.

*Inidhamishe akili kuwa makini Wakati wa kuomba—Maombi ya kila siku ni muhimu katika ukuaji wa neema, na hata kwa maisha ya kiroho yenyewe, kama vile chakula cha muda cha hapa duniani, tunachokula kwa ustawi wa kimwili. Tunapaswa kujizoesha kuinua mawazo kwa MUNGU katika sala. Akili ikimangamanga huko na kule, lazima tuirudishe; kwa jitihada za dhati na zenye uvumilivu, mazoea hatimaye yatafanya iwe rahisi.


---

Ni nani alitoa ushindi wa Yeriko? Aliwaambia wafanyeje ili ukuta uanguke? Ni nani aliwapa wana wa Israeli chakula? Ni chakula gani walilima? Je, amiri wa jeshi la BWANA ni nani na alimwambia nini Yoshua? Wapelelezi wawili walirudi kwa Rahabu kufanya nini?

**SIKU YA 57**
**(Februari 26)**

# Dhambi ya Akani, Hakuna mtu Ambaye ni Kisiwa

**-Yoshua 7**



Basi wana wa Israeli walipoona Yeriko imeanguka, bila shaka waliamini watamaliza nchi zote kwa kasi. Kutoka Yeriko walienda kupigana na mji mdogo wa Ai. Yoshua alituma watu ili kuipeleleza nchi. Basi wakaleta ripoti kwamba mji wa Ai "watu ni wachache" asitaabishe wanajeshi wote kwenda. Wala hakuna haja ya wote kwenda ila watu 2000 au 3000 tu. Watu hawa siku hizo walikuwa hawana bunduki wala makombora.

Wale watu walipoenda vitani, walipigwa sana, kisha watu 36 wakauawa na waliobaki wakakimbia. Walipofika kwenye mtelemko, mioyo ya watu iliyeyuka ikawa kama maji kwa woga. Yoshua alipowaona alirarua mavazi yake huku akiwa amefadhaika sana na kuanguka kifudifudi mbele ya sanduku la Agano la BWANA mpaka jioni, yeye, na wazee wa Israeli. Wakatia mavumbi vichwani mwao. Yoshua akamwuliza BWANA aliyewavusha mto Yordani, kwa nini amewavusha aje kuwatia mikononi mwa Waamori kuwaangamiza. Akasema, "Laiti tungelikuwa radhi kukaa ng'ambo ya Yordani." Akasema baada ya Waisraeli kukimbia adui zao, wenyeji wakisikia

habari hizo, watawazingiria na “kulifuta jina letu katika nchi. Nawe utafanya nini kwa ajili ya Jina Lako kuu?”

BWANA alimjibu Yoshua, “Haya inuka mbona umeanguka kifudifudi.” Akamwambia Israeli wamefanya dhambi, wamevunja agano Lake kwani wametwaa baadhi ya vitu vilivyoweka wakfu; tena wameiba, na kuvificha na kuvitia pamoja na vitu vyao wenyewe. Hii ndiyo sababu walishindwa kusimama mbele ya adui zao na kuwapa visogo kwa maana wamelaaniwa. BWANA akawaambia hatakuwa pamoja nao tena wasipokiharibu kitu kile walichoiba kilichokuwa wakfu. Yoshua Akaambiwa ainuke na kutakasa watu wote wawe tayari kesho yake. Mungu akamwambia wazi “kitu kilichowekwa wakfu kiko katikati yako” na hawataweza kusimama mbele ya adui mpaka wakiondoe. Pengine Akani alikuwa amejificha hemani mwake akififikiri hakuna ajuaye uovu wake.

Asubuhi yake watu wangeliletwa kwa kufuata makabila yao, na kisha lile kabila lililotwaa vitu vilivyo wakfu, wataletwa ukoo kwa ukoo na kisha mtu kwa mtu. Naye aliyetwaa vitu vilivyowekwa wakfu atapigwa mawe na kuteketezwa kwa moto, yeye na vitu vyote alivyo navyo kwa kuwa amelivunja agano la Bwana na kutenda upumbavu katika Israeli. Akani alikuwa hayuko tayari kuomba msamaha, na hakuangalia kwamba alikuwa anawadhuru wengine kwa tabia yake ya tamaa,

Basi Yoshua aliamka asubuhi na kufanya kama alivyoagizwa. Makabila yakapita na kabila ya Yuda ikatwaliwa. Katika kabila la Yuda walitwaliwa ukoo wa Wazera. Kisha mtu kwa mtu na Akani akatwaliwa. Yoshua akamwuliza, “Akani mwanangu, nakusihi umtukuze BWANA Mungu wa Israeli ukaungame Kwake uniambie ulilotenda wala usinifiche.” Akani alisema ni kweli amefanya dhambi, juu ya BWANA Mungu wa Israeli na akaeleza kwamba alichukua joho zuri la Babeli na shekeli mia mbili za fedha na kabari ya dhahabu, uzani wake shekeli hamsini. “Nalivitamani nikavitwaa; tazama, vimefichwa mchangani katikati ya hema yangu na ile fedha chini yake.” Yoshua alituma watu wakapiga mbio hemani kwa Akani na kutoa vitu vilivyofichwa na kuvileta kwa Yoshua. Walimtwaa Akani na vile vitu, mifugo yake, watoto wake na vyote alivyokuwa navyo wakavileta. Yoshua akasema “mbona umetufadhaisha hivi? Bwana atakufadhaisha wewe leo.” Basi alipigwa kwa mawe, yeye na familia yake, na juu yake wakakusanya mawe na kuyaweka juu yake. Hata nasi hatuwezi kuficha dhambi zetu leo, Mungu atusaidie tuziungame na kuziacha.

Baada ya hayo walienda Ai na wanajeshi 30,000 na kuutwaa mji, kwa kufuata maagizo ya BWANA. Waliwavizia na kukimbia kama waliposhindwa kwanza. Walipotoka kuwafuatia, watu waliokuwa wakivizia waliingia Ai na kuuteketeza mji na moto. Watu wa Ai walipoona mji wao umeteketezwa hawakuwa na pa kukimbilia kwa vile walikuwa wamezingirwa. Mungu akaitia Ai mikononi mwao. Yoshua akajenga madhabahu ya Bwana katika mlima Ebali na kutoa sadaka ya shukurani. Kuna masomo mengi sana katika sura hii. Kwanza, haikuonekana kwamba Yoshua aliomba ushauri kwa Mungu wakienda Ai, alichukulia jambo hilo kirahisi kwa sababu ulikuwa mji mdogo, naye alipoona janga hilo alichanganyikiwa na kuogopa na kisha akamuuliza Mungu kwanini haya yamewatokea, ndipo akamimina moyo wake. Ni Mungu Ndiye alikuwa msaada wao na sio ushujaa wao. Akani naye

hakuchukua amri ya Mungu kwa uzito na hivyo kusababisha uharibifu kwa taifa na familia yake. Dhambi huleta matokeo mabaya sana, na tunahitaji msaada wa Mungu kila dakika ya siku ili kuchukua hatua zozote zinazohitajika ili kuiepuka. Eh Bwana Yesu tunakuhitaji ili tuishi maisha yasiyo na dhambi katika ulimwengu wetu huu uliochafuliwa. Sote tunapaswa kuvaa silaha za vita za Waefeso Sita. Hebu tuwe chanzo cha baraka kwenye familia zetu na siyo chanzo cha matatizo, Je, unakubaliana nami? Hakuna mtu aliye kisiwa, uamuzi wetu unaathiri wengine. Kila mtu anapaswa kumtegemea Mungu kuwa mshauri wake. Akani alitanguliza masilahi yake mwenyewe juu ya yale ya wengine, na uchaguzi wake ukaua askari 36 na kutia aibu kazi ya Mungu.

Uamsho wa kweli na matengenezo yanayoongozwa na Roho Mtakatifu hugeuza akili zetu kuakisi nia ya Kristo. Kinachovutia asili yetu ya dhambi kinakuwa si muhimu tena. Malengo yangu makuu ni kumpendeza Mungu aliyeniumba na kuwabariki wengine ambao ni kaka na dada zangu katika Kristo. Kamwe tusichelewe kuungama dhambi, tukingoja mpaka mambo yaharibike, na pia tuepuke kutamani vitu vya jirani zetu. Mafanikio hayawezi kuja kama tuna dhambi kambini. Tuombe kumpendeza Mungu "Mwatamani, wala hamna kitu, mwaua na kuona wivu, wala hamwezi kupata. Mwafanya vita na kupigana, wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi! Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu" Ni lazima tufuate mipango Yake Mungu na si kudhani kuwa Yeye Ndiye aifuate mipango yetu. Tukeshe na kusali, tukiuliza kwenye kila hatua, "Bwana nifanyeje kuhusu jambo hili?"; "Tafadhali nionyeshe ninachokosa, na unifunulie mapenzi Yako" Hebu sala zetu zifike juu mbinguni na si kwenye paa la nyumba yetu tu! Ushawishi unaopaswa kuogopwa zaidi kanisani si ule wa wapinzani wa wazi, makafiri, au wanaotukana kanisa, bali ni wale wanaomkiri Kristo kwa mdomo ila wanatenda kinyume. Hawa ndio wanaozuia baraka za Mungu wa Israeli na kuleta udhaifu juu ya watu wake. Dhambi inapoungamwa Mungu huchukua makosa ya mwanadamu na kuyageuza kuwa baraka.

*Ombi halihitaji Kuwa refu au kuwa la sauti ya juu au kugumia—Kusali hakueleweki jinsi inavyopaswa. Maombi yetu hayapaswi kumjulisha MUNGU juu ya kitu ambacho hajui. Bwana anajua siri za kila roho. Maombi yetu hayapaswi kuwa marefu na yenye sauti kubwa. MUNGU anasoma mawazo yaliyofichika. Tunaweza kuomba kwa siri, na Yeye anayeona katika siri atasikia, na atatupatia thawabu hadharani.

---


Kwa nini Yoshua alianguka kifudifudi? Dhambi ya Akani ilikuwa nini na nani alimwona akiifanya? Mungu alimwambia Yoshua afanye njia gani kumtafuta mkosaji? Kwa nini kutamani ni dhambi? Yoshua alimwambia Nini Akani? Kwa nini familia yake iliangamizwa pia? Watu wangapi walifanikiwa kuiteka Ai? Kisa hiki kinatufundisha nini? Vitu vya Yeriko vilikuwa mali ya nani? Kwa nini amri ya 10 ni ngumu kujulikana kwamba tunaivunja?

**SIKU YA 58**
**(Februari 27)**

# Yoshua Adanganywa na Wagibeoni na Jua Lasimama

**- Yoshua 10-21**

Wakanaani walikaa katika falme ndogo ndogo nyingi. Wakati huo huo wenyeji wa Gibeoni walipoona jinsi mataifa yanavyoyeyuka kwa Waisraeli, Wagibeoni walifanya mkutano na kutenda hila. Wakaenda kwa Israeli wakijifanya kuwa na ujumbe. Walichukua punda na magunia ya kuchakaa, viriba vya maji vikuukuu na vyenye viraka, viatu vilivyotoboka na kushonwa na nguo kuukuu. Tena wakachukua mikate iliyovunda. Walipofika kwa Waisraeli walimwendea Yoshua na kumwambia kuwa wametoka nchi ya mbali sana, na wangetaka wafanye Agano Naye. Kwanza Yoshua aliwashuku kwamba wanakaa karibu na watawezaje kufanya maagano nao, ndipo wakasema, "sisi tu watumishi wako, tumesikia sifa za BWANA Mungu wako na hayo aliyowafanyia Wamisri na Sihoni na Ogu pamoja na raia Wake. Wakasema viongozi wao waliwaambia kwamba wachukue vyakula na kwenda kuwalaki Waisraeli na kujisalimisha kwao.



Yoshua hakumwuliza BWANA ukweli wa hawa Wagibeoni na hivyo akafanya agano nao. Hata leo hiyo bado ni shida yetu, tunafanya vitu bila kumwuliza BWANA kwa njia ya sala, na kwenda kinyume cha maagizo Yake na tukipata shida ndipo tunamrudia Yeye. Baada ya siku tatu Waisraeli wakagundua kwamba Wagibeoni ni waongo kwani baada ya kusafiri siku tatu wakaifikia miji ya watu hao. Wana wa Israeli hawakuwapiga Wagibeoni kwa vile walikuwa wameshawaapia kwa BWANA, Mungu wa Israeli kwamba hawawezi kuwagusa hao. Wakuu wakawapa adhabu ya kuwa watumishi wao kwa kuteka maji, na kupasua kuni, kwa ajili ya mkutano wote. Yoshua aliwaita na kuwaambia "mbona mmetudangaya." Wao walijibu kwamba walikuwa na woga, kwani walijua kuwa BWANA amewapatia nchi kama alivyomwamuru mtumishi Wake Musa. Wakawa tayari kufanya kazi hii ya kutumwa, "Tazama sisi tu mkononi mwako, basi kama uonavyo kuwa ni vyema na haki kwako wewe kututenda, tutende hivyo. Basi Wagibeoni wakateka maji ya mkutano, na ya madhabahu kwa miaka mingi. Kule tu kufanya kazi kwenye madhabahu ni mbaraka kwani waliona jinsi picha ya wokovu ilivyo, na wengi wetu tunafikiri watu wa mataifa hawakuruhusiwa kamwe kuingia hekaluni ila hapa tunaona walipata nafasi ya kumfanyia Mungu kazi kwa njia ya ajabu kwani uwepo wa Mungu upo hapo!

Mfalme wa Yerusalemu Adoni-sedeki aliposikia kuwa Yoshua ameushika Ai na kuuharibu kabisa kama Yeriko na wenyeji wa Gibeoni wamefanya amani na Waisraeli japo mji wao ulikuwa mkubwa na watu wake wote walikuwa mashujaa; alituma ujumbe kwa wafalme wengine wanne, jumla wakapata falme tano za Waamori ili kuipiga Gibeoni. Wagibeoni walituma ujumbe kwa Yoshua kule Gilgali wakisema, "usiulegeze mkono wako hata ukatuacha sisi watumishi wako; uje kwetu kwa upesi utuokoe, na kutusaidia." BWANA akampa ruhusa Yoshua kwenda huko, basi Yoshua alitembea na jeshi usiku kucha na kuwafikia, kisha Bwana akawatapanya nao wakauawa na wengine wakakimbia mbele ya Israeli. Wengine wengi zaidi walipigwa kwa mvua ya mawe au barafu. Vita ikiwa inaendelea Yoshua akaona giza linaingia, ndipo alipomwomba Mungu na kutamka "wewe jua simama" ndipo jua likasimama na mwezi ukatulia hata Waisraeli walipokuwa wamewashinda adui zao. Ilitokeaje? Hatujui, lakini Mungu Ndiye aliyeumba jua, na hivyo anaweza kuliamrisha. Jua lilisimama katikati ya mbingu, wala halikufanya haraka kuchwa kama muda wa siku nzima. Mwezi nao ukasimama, wala hakuna siku nyingine mfano wa hiyo siku za nyuma au mbele, "BWANA kusikia sauti ya binadamu." BWANA aliwapigania Israeli. Wafalme watano wakakimbia wakajificha kwenye pango la Mekida na Yoshua alipopata habari hiyo aliwaambia wazibe mdomo wa pango kwa mawe makubwa. Yoshua aliwaamuru tena kufungua mlango wa pango na wafalme watano wakaletwa na kuadhibiwa. Na hivyo Israeli ikamalizia kwa kupiga watu wote kwenye miji hii na hizi falme tano yaani Yerusalemu, Hebroni, Lakishi, Yarmuthi na Egloni, zikawa za Israeli.

Basi kila mtu aliyeishi wakati huo kule Palestina, alijua kwamba jua limesimama. Mungu aliingilia kati. Yoshua na jeshi lake hawakuwa na nguvu. Nasi tusijaribu kupigana vita vyetu kwa nguvu zetu wenyewe, tumtumaini Mungu kwa uingiliaji kati usio wa kawaida.

Je, unaamini kwamba Mungu bado anatenda miujiza? Basi mtazame Yeye kwa imani, ni Mungu atendaye. Muujiza huu mkubwa unashuhudia kwamba uumbaji uko chini ya udhibiti wa Muumba. Shetani anatafuta kuficha kutoka kwa wanadamu ukuu wa Bwana katika ulimwengu ila, wakati ubinadamu unashirikiana na Uungu matokeo ni ushindi wa kudumu. Yoshua alifanya sehemu yake kama kiongozi na alitegemea kabisa ahadi ya Mungu kwake naye hakuogopa. Yoshua alizungumza na jua, nalo likasimama na mwezi ukasimama. Tunapotembea na Bwana katika nuru ya Neno Lake tutatimiza yasiyowezekana. Bwana halegei katika ahadi zake. Ombi letu la leo ni kwamba Bwana atupiganie vita vyetu nasi tutasimama tuli na kuuona wokovu wa Bwana. Asante Bwana kwa kupigana vita vyetu na kwa ushindi. Kwa kuwa Bwana ulikuwa tayari kusimamisha jua kwa siku nzima ili watu wako watimize kazi ambayo ulikuwa umewapa, Wewe Uko tayari pia kufanya muujiza wowote unaohitajika ili kutusaidia kumaliza kazi ya kueneza injili ulimwenguni. Anatamani sana kuona kazi imekamilika. Hebu tushirikiane Naye!

Yoshua akaigawa nchi baada ya mapigano kwa kila kabila, Walawi hawakuwa na urithi wa nchi maana walikuwa na kazi ya wakfu. Wakaweka miji ya kukimbilia kwake yeye amwuaye mwenzake kwa bahati mbaya. Wasingemtoa pale yule aliyeua mpaka kifo cha kuhani mkuu. Naye Yoshua mwana wa Nuni akapata urithi wa

mji alioutaka katika vilima vya Efraimu, uliokuwa mahame, akajenga na kukaa huko. Alionesha kutokuwa na ubinafsi wa kujichagulia vitu vizuri vizuri. Walawi nao wakapata miji mwishoni wakakaa na wakawa na mifugo yao. Yoshua anasema "halikuanguka Neno lolote katika jambo lolote lililokuwa jema ambalo BWANA alikuwa amelinena katika habari ya nyumba ya Israeli, yalitimia yote" na hata kuzidi yale aliyoahidi. Kitabu cha Jasheri chapatikana mtandaoni na katika sura ya 88 kimeelezea jambo hili!

Twamwona Kalebu akiwa na miaka 85 akiwa na nguvu zake, akasema apewa mlima (Yoshua 14:12) Ahadi ambayo alipewa akiwa na umri wa miaka 45 ilitimizwa akiwa na umri wa miaka 85 kwa sababu bado alimpenda na kumtumikia Mungu.
Somo kwetu ni kwamba kile ambacho Bwana ameahidi hakika kitatimia, tunahitaji tu kuwa na subira, tumwamini na kumtii Mungu. mapenzi Yake hakika yatatimia.
Binti yake Aksah hakuogopa kumwomba babaye shamba, na baadaye aliolewa na mwamuzi Othinieli. Nasi leo tusisite kumwomba Baba yetu wa Mbinguni, Huo ulikuwa ni mpango wa Mungu kwa Israeli kwa kila mtu apate kipande cha ardhi ili kuepuka umasikini na kujifunza kazi.

*Hatupaswi Kujaribu Kumwamuru MUNGU Katika Maombi—Maombi yetu hayapaswi kuwa katika namna ya amri, bali yawe ni ya maombezi/maombi, Kwake Yeye, ili Ayafanye mambo tunayotamani kutoka Kwake.

---

Kwa nini Yoshua alidanganywa? Adhabu ya Wagibeoni ilikuwa nini? Wafalme watano walikuwa wa mataifa yapi? Kwa nini Jua lilisimama? Yoshua alisema Mungu ametunzaje ahadi Zake? Ni kosa gani Yoshua na wazee walifanya? Waliamuaje kesi ya Wagibeoni? Wagibeoni walionaje kuhusu hili? Kwa nini ni muhimu kumwuliza Mungu cha kufanya na kumruhusu atawale kila jambo hata lile dogo la maisha yetu?

**SIKU YA 59**
**(Februari 28)**

# Siku za Mwisho za Yoshua

**- Yoshua 21-24**

Mzee Kalebu na Yoshua walikuwa ukingoni mwa Yordani, tayari kuvuka mara ya kwanza, lakini ilibidi warudi na watu kwa miaka 40 japo sio wao waliofanya makosa. Sasa walikuwa wanagawa Kanaani baada ya kuzunguka jangwani. Kalebu alikuwa mzee wa miaka 85 sasa. Shujaa huyu wa vita aliomba apewe mlima aweze kuukomboa. Mlima ulikuwa ni Hebroni uliokuwa unakaliwa na Waanaki, naye akautwaa. Alisema kwamba yeye atakayesaidia kuutwaa mji mwingine uitwao Kiriath-seferi atampa binti yake Aksa kuwa mkewe. Othnieli aliyekuwa mwamuzi wa kwanza, aliutwaa mji na akapewa Aksa, na Aksa akamwomba baba yake ardhi yenye chemchemi ya maji akapewa. Yoshua na Kalebu hawakuuliza mahali penye rutuba au pazuri, hawakuwa na uchoyo japo ndio waliokuwa wazee kupita wote. Mungu alitaka kila mtu awe na mahali pa kulima, ili kusiwe na umasikini na pia kilimo ndiyo alfabeti ya elimu. Binadamu yoyote hapaswi kuogopa kilimo kamwe. Mbinguni watu watakuwa na nyumba kwenye mji wa Yerusalemu, na pia watakuwa na nyumba nje ya mji au vijijini na huko kila mmoja atakuwa na mahali pa bustani. Ndiyo ulikuwa mpango wa Mungu kutoka Edeni. Adamu alikuwa mfalme ila ndiyo jambo la kwanza aliloambiwa hata kabla ya kupewa mke, aitunze bustani. Ila kazi hiyo haitatoa jasho na itaburudisha moyo sana kuona vitu vikikua na bustani ikipendeza na mazao ya chakula na maua! Ombi letu la leo ni kwamba Mungu atujalie neema ya kuendelea kuwa waaminifu hadi mwisho maana Yeye aliyeahidi ni mwaminifu na hakika atatimiza. Maadamu tunaendelea kuwa waaminifu Kwake Bwana kama alivyoagizwa wokovu wetu ni hakika. Kupiga kura ili kuamua mambo muhimu, si jambo linalopaswa kufanywa leo kwenye kila shuguli, kwani hatuongozwi Naye kwa jinsi ile siku hizi. Yabidi tuombe, na kuwe na kamati ya wajumbe walioteuliwa kwa kuchujwa, hawa ndiyo hupiga kura kwa niaba ya wengine, wote tukifanya maombi ya dhati kwamba mapenzi ya Mungu yatimizwe, Naye Mungu hakika ataliongoza kanisa Lake.

Yoshua alikumbuka kuweka miji ya kimbilio, kama Musa alivyozungumza naye. Miji sita ilitengwa, mitatu ngambo ya mto Yordani, na mitatu baada ya kuvuka Yordani, kwa yule anayeua mtu kwa bahati mbaya. Sehemu hizi zilifahamika vyema na zilikuwa rahisi kufikika kwa mwendo wa siku moja hivi, na pengine zilikuwa milimani ili zionekane. Sheria hii ilifundisha watu kuwa na uvumilivu na kujitawala nafsi, ili kumlinda mtu asiye na hatia, au aliyeua bila kudhamiria. Tunahitaji kutunza haki bila kuhamaki kwa hasira za ghafla au kutaka kulipiza kisasi. Mfano wa kuua bila kudhamiria ni baadhi ya ajali za barabarani, watu wanaoangusha mti na kisha ukamwangukia mtu kwa bahati mbaya.

Watu wengi wameuliza kwanini Mungu Mwenye upendo awaangamize hawa watu wa Kanani? Watu hawa wa Kanani walipewa muda wa majaribio kwa miaka 400,

yaani mlango wa rehema ulikuwa wazi kwao, lakini walikuwa wameshikamana na ibada yao ya sanamu nao wangekuwa na ushawishi mbaya kwa Waisraeli na watu wengine pia. Hakika Yoshua alitekeleza hukumu ambayo walijiletea juu yao wenyewe. Yoshua alitwaa miji yote ya wafalme hao, na wafalme wao wote, akawapiga kwa makali ya upanga. Akawaangamiza kabisa, kama Musa mtumishi wa BWANA alivyoamuru."Yoshua 11:12. Kwa nini basi Mungu alitoa maagizo haya kwa Musa? Mlango wa rehema wa Wakanaani ulikuwa umefungwa. Kama Mungu alivyomwambia Ibrahimu, Wakanaani (pia waliitwa Waamori) wangepewa kipindi cha majaribio ambacho kingechukua miaka 400. Mwishoni mwa kipindi chao cha majaribio, wangeangamizwa ( Mwanzo 15:13-16). Hakika kumbe kuna kiwango maalum cha uovu ambacho mataifa yakipitiliza, Mungu hutoa hukumu. . . Kama wakati wa gharika, wakati wa Sodoma, au wakati wa Kanaani, walitawaliwa na tamaa mbaya na misukumo iliyowapeleka kutenda ukatili wa hali ya juu. Tunasoma kuhusu kutoa watoto wao dhabihu, ibada za nyoka, na kufanya mambo ya uasherati katika mahekalu yao. Mahali Patakatifu pao palikuwa na makahaba maalumu wa jinsia zote. Na Mungu alivumilia haya kwa miaka 400! Je, unaweza kufikiria ni watoto wangapi waliochomwa moto wakiwa hai katika miaka 400? Hakika Mwenyezi Mungu alikuwa na huzuni na subira. Vyombo vya habari leo vimetuelezea matukio mengi yanayofanana na haya mfano kutekwa nyara kwa watoto, kuuwawa na kubakwa na kundi la Boko haram na kwenye miji yenye vita nk. Cha kukumbuka zaidi ni kwamba Mungu ni Mwenye haki na rehema daima, na mara zingine watu wachache hufa, ili kuzuia wengi zaidi wasife. Maana binadamu ambaye daima anawaza maovu, akiachiwa afanye anachokitaka, na silaha alizo nazo na uovu moyoni, bila mipaka, atafanya vitu vya kutisha mno, asipotawaliwa na Roho wa Mungu. Mungu si dhalimu, tumtumaini na kumtegemea Yeye, na siku moja atatueleza kile alichokuwa anakabiliana nacho, nasi kama watoto wachanga. tusiojua changamoto za Baba yetu mwema, tutulie miguuni Pake, tukijua anatutakia mema, na anashugulikia mambo yote kwa wema wote unaowezekana na siku moja, dhambi haitainua pembe zake tena!

Kiwango cha uovu ambacho ulimwengu wetu wa sasa hauwezi kupitiliza kimewekwa na Mungu. Kwa sasa, Mungu anavumilia kuona maovu mengi yanayotendeka katika ulimwengu wetu—ambao unazidi kujaa jeuri. Hivi karibuni, katika Kilio Kikuu, watu wa Mungu watatoa onyo la mwisho, wakisema, "Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msije mkashiriki dhambi zake, na msije mkapokea mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake- Ufunuo 18:4-5. Baada ya hayo, "siku ya Bwana itakuja kama mwivi wakati wa usiku, ambayo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitayeyuka kwa joto kali; dunia na kazi zilizomo ndani yake zitateketezwa." 2 Petro 3:10. Tusisahau kwamba Mungu ambaye ataiangamiza dunia, ni Mungu Yule Yule aliyeshuka chini hapa na kufa juu ya msalaba wa kikatili ili kuuokoa ulimwengu. Kuangamiza Kwake ulimwengu hakumaanishi kwamba upendo Wake ulikuwa mdogo kuliko alipokuja kufa kwa ajili ya kila mwanadamu,la! Yeye ni mkamilifu na Yeye ni upendo. Siyo kwamba Yeye anao upendo tu, bali, Yeye ni Upendo.

Yoshua alipokuwa mzee aliwaita watu kama ambavyo Musa alifanya kabla ya kufa kwake. Akarudia historia ya Ibrahimu toka Uru wa Wakaldayo, mpaka Israeli

kwenda utumwani, kukombolewa na kupita bahari ya Shamu, na miujiza yote ya ajabu ya Mungu ya ushindi. Aliwaita Wareubeni, Wagadi na Nusu ya Manase na kuwaambia kwamba walikuwa wameshika mausia ya BWANA na sasa walikuwa na ruhusa kurudi ngambo ya pili ya Yordani kwenye miji yao. Na kwamba "mjibidishe sana kuzifanya amri na sheria ambazo Musa mtumishi wa BWANA aliwaamuru, kumpenda BWANA Mungu wenu na kuenenda katika njia Zake zote, na kuzishika Amri Zake na kushikamana na Yeye na kumtumikia kwa moyo wenu wote na nafsi zenu zote." Yoshua akawabariki na kuwapa ruhusa warudi kwao na nyara (ng'ombe, shaba, dhahabu, fedha, chuma na mazao) na kisha wagawane na ndugu zao.
Makabila haya mawili na nusu ng'ambo ya Yordani, walijenga madhabahu kubwa walipofika kule, wakati madhabahu ilikuwa iwe moja tu pale walipoishi Walawi. Makabila yaliyosalia ya Israeli waliposikia haya, walikutanika Shilo madhabahu ilipo na kutuma ujumbe. Finehasi kuhani (mwana wa Eliazeri na mjukuu wa Haruni) na watu kumi ambao ni viongozi wakaenda na kuwauliza "Ni kosa gani mlilolikosa juu ya Mungu wa Israeli… hata mkajenga madhabahu na kuasi hivi leo juu ya BWANA?" Ingekuwa vizuri kumwuliza kuhani kabla ya kufanya jambo hili la kujenga. Waliwakumbusha ndugu zao na kusema, "ule uovu wa Baal-peori" kwa Baalamu haututoshi? BWANA akiwakasirikia kwa kumwacha na kugeuka atatukasirikia sote Israeli. Wakawasihi wasimwasi BWANA, wala Israeli kwa kujenga madhabahu zaidi ya hiyo ya Israeli. Wakakumbusha kwamba dhambi ya Akani ilileta maafa kwa wengi, zaidi ya Akani mwenyewe. Wana wa Reubeni, Gadi na nusu ya Manase walijibu, "Mungu, BWANA Yeye anajua kama ni uasi na kukengeuka kuacha kumwandama Yeye." Wakasema ni ushahidi kwao na watoto wao, wa ibada kwa Mungu. Walisema madhabahu hii si ya kuteketeza wala ya sadaka yoyote ila ushahidi kwa vizazi vijavyo kuhusu BWANA wa Israeli. Finehasi kuhani akasema amejua sasa, "vinginevyo wangefanya ndugu zao Waisraeli wawaadhibu. Finehasi, na Israeli wakaendelea kumwabudu Mungu wakati wa Yoshua. Baada ya vita vya kumiliki nchi, Shilo pakaendelea kuwa mahali pa kuabudia wakati Yoshua alipokuwa hai.

Yoshua aliwaita watu na kuwaambia, "mimi sasa ni mzee, … iweni mashujaa kuyashika yote yaliyoandikwa kwenye torati, myatende na msiyaache kwa kugeuka kuume au kushoto, msitaje miungu ya mataifa hayo au kuitumikia au kuiabudu. BWANA amewafukuza mbele yenu mataifa hodari, na yenye nguvu. Mtu mmoja miongoni mwenu atafukuza watu elfu, na wawili watafukuza kumi elfu. Maana BWANA anawapigania kama alivyoahidi, mpendeni Mungu wenu. Ila mkirudi nyuma na kushikana na mataifa na kuoana nao, na kuingia kwao na wao kuingia kwenu, hakika Mungu hatawafukuza tena mbele ya macho yenu bali watakuwa mtego, tanzi na mjeledi mbavuni mwenu, na miiba machoni penu." "Angalieni mimi leo naenda njia ile waendayo watu wote wa ulimwengu." Mungu amewapa nchi msiyoitendea kazi, mnakula msivyovipanda na miji msiyoijenga, basi mcheni BWANA kwa unyofu. "Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia BWANA, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu waliitumikia ngambo ya mto, au kwamba ni miungu ya wale Waamori … lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia BWANA." Alikazia kiongozi msaidizi huyu wa jemedari wa jeshi la Israeli. Watu walijibu kwa haraka kwamba tutamtumikia BWANA. Walisema haraka wakimaanisha, lakini hawakuishi hivyo. Ndiyo shida yetu hata siku za leo,

hebu tuombe neema ya kusema na kutenda. Yoshua alifanya agano na ahadi nao na kuwa amri na agizo huko Shekemu, akaweka jiwe kubwa la agano kati yao.

*Omba kwa Imani—Omba kwa imani. Hakikisha unayapatanisha maisha yako na maombi yako, ili upate kupokea baraka ambazo unaziombea. Usiache Imani yako isidhoofike, kwani baraka zinazopokelewa zinalingana na imani iliyopo, yaani inayozoezwa. "Na iwe kwako kulingana na imani yako". Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata." Mathayo 9:29; Mathayo 21:22. Omba, amini, furahi. Mwimbieni MUNGU sifa kwa sababu amejibu maombi yenu. Muendee kwa Neno Lake. "Yeye ni Mwaminifu aliyeahidi." Waebrania 10:23. Hakuna ombi hata moja la dhati linalopotea. Njia iko wazi; na mkondo unabubujika. Umebeba miliki ya uponyaji, ukimimina mawimbi ya kurudisha uzima, afya na wokovu.

*Hebu unyofu wa moyo, kuwa dhati na imani iwe sifa ya maombi yenu. Bwana Yuko tayari kutufanyia "mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo." Waefeso 3:20. Zungumza hilo; liombee hilo. Usiongee kuhusu kutokuamini. Hatuwezi kumudu kumuachia Shetani aone kwamba ana uwezo wa kuzitia nyuso zetu giza na kuhuzunisha maisha yetu.

---

Othnieli anakumbukwa kwa jambo gani? Kwa nini Waisraeli walihamaki waliposikia madhabahu imejengwa Shilo? Miji ya makimbilio ilikuwa na kazi gani? Kwa nini kutoa mioyo yetu kwa BWANA ni muhimu?

**SIKU YA 60**
**(Februari 29)**
**LEAP YEAR**

# Waamuzi - Yoshua 24 na Waamuzi 1

## Chagueni Ninyi Leo.

Mungu alifanya agano na Israeli kwenye Mlima Sinai (Kut. 19:3-6 na 20:1-7), na Musa akalifanya upyaAgano hilo pamoja nao kabla ya kufa (Kum. 29 na 30). Katika sura hiiYoshua pia anafanya upya agano kabla ya kifo chake kinachokaribia. Yoshua anawahimiza wana wa Israeli kumchagua Bwana kuwa Mungu wao milele. Mara tatu wanaweka nadhiri ya kuwa waaminifu kwa Bwana (24:16, 21, 24). Kisha Yoshua anaandika mambo haya katika Kitabu cha Sheria na kusimamisha mnara wa jiwe kama ushuhuda wa nadhiri yao (Fungu la 26-27). Watu walitunza ahadi zao muda wote walioishi, wale wote waliokuwa wameona kile ambacho Bwana alikuwa amewafanyia.

Leo pia tunapaswa kukumbuka karama nyingi ambazo Bwana ametupa. Yesu alikuja kuishi na kufa kwa ajili yetu. Akawa Mpatanishi wetu mbinguni. Aliahidi kwamba atarudi na kutupeleka kwenye Nchi yetu ya Ahadi ya mbinguni. Tunapaswa kuzipitia upya karama Zake alizotupa, mara kwa mara tukiwa na moyo uliojaa shukrani tufanywe upya kwa kujitolea kwetu Kwake. Basi Yoshua akawabariki na kisha alikufa akiwa na miaka 110 kama Yusufu, wakamzika kwenye mji wake wa Timnath Sera. “Nao Israeli walimtumikia BWANA siku zote za Yoshua na wazee walioishi baada ya kufa kwake Yoshua; yaani hao walioijua kazi yote ya BWANA aliyowatendea Israeli. Eleazari kuhani mkuu naye akafa naye Finehasi akaanza kazi ya kuhani mkuu.

Inaonekana kuwa Waisraeli walichoka kuwafukuza adui zao na kuteketeza miungu yao. Walipaswa kufanya sehemu hii ya Palestina kuwa takatifu na ya matendo ya haki, ndipo wangeng’aa na kuonesha utukufu wa Mungu kwenye nchi ya uovu. Kabila la Yuda liliwafukuza watu wa milimani. Yoshua alipokufa walimfuata “Adoni Bezeki” mfalme katili wa Wakanaani na wakamkata vidole vyake vya miguu na mikono yake naye akakiri kwamba ameua wengi na kuwafanyia ukatili. Wana wa Yuda wakapigana na kuutwaa mji huo wa mlima bali kwenye bonde hawakufanya vile wakiogopa kwamba “wana magari ya farasi ya chuma.” Walisahau kuwa Mungu Ndiye aliwapigania na si nguvu zao au farasi wa chuma. Sura ya kwanza ya kitabu cha Waamuzi inaonesha kuwa makabila ya Manase, Efraimu, Zabuloni, Asheri, Naftali, hawakuwafukuza wenyeji wa pale. Malaika wa BWANA akakwea kutoka Gilgali kwenda Boakimu “mahali pa waliaji” na kuwaambia kwamba BWANA aliahidi kutolivunja Agano Lake ila waivunje na kuiangusha miungu ya wenyeji wa nchi ile “lakini hamkusikia sauti Yangu, je, ni kwa sababu gani? Basi malaika akasema kwamba kwa sababu hiyo adui zao hawatafukuzwa lakini watakuwa kama miiba mbavuni mwao. Watu waliinua sauti na kulia na wakamchinjia Bwana sadaka

huko.

Lakini kiliinuka kizazi kingine nyuma yao cha watu ambao “hawakumjua BWANA wala kazi ambayo alikuwa ameitenda kwa ajili ya Israeli. Wakamwacha Bwana aliyewatoa Misri na kufuata miungu ya Baali na Maashtorethi ya watu waliokaa karibu nao na kujiinamisha mbele Yake. Walimkasirisha na kumghadhabisha BWANA, na hasira Yake ilipowaka akawauza na kuwatia katika mikono ya maadui pande zote. Kila walikokwenda ilikuwa shida, mpaka wakafadhaika sana. Ndipo BWANA alipoinua Waamuzi ili kuwaokoa watu Wake, ila hawakusikiliza hao Waamuzi maana walifanya uasherati kwa kufuata miungu mingine na kujiinamisha kwao. Mungu anasema mtu anayeabudu miungu mingine ni kama mke aliyemwacha mume wake na kwenda kwa mwanamume mwingine. Baada ya kufa mwamuzi mmoja Israeli walijiingiza matopeni na kujichafua tena kwa uovu kuliko baba zao kwa kuifuata miungu mingine na kuitumikia, bila kuacha matendo ya ukaidi na kumsahau Mungu kwa upesi. Walioa binti za watu hawa na kuwaoza binti zao. Jambo hili la kuoa mtu asiyemwamini Mungu ni gumu sana maana linafanya watu wengine wamwache Mungu. Ni wachache sana wanaweza kupigana vita vya nyumbani mwao. Wanaweza kuwa mashujaa wa vita nje ila nyumbani mwao wanajisahau na Shetani anawanyemelea na kuwateka.

Lakini hili ni fundisho kwetu sote kwamba tusimwache BWANA. Ni rahisi kuahidi kumtii BWANA wakati tupendao na kuasi wakati tunapotaka, ila BWANA anataka tuwe waaminifu na kumtegemea Yeye siku zote. Mtu hujiuliza ilikuwaje wana wa Israeli waliokuwa na historia tajiri sana iliyojikita katika Mungu waliweza kumpa kisogo Bwana. Bwana atusaidie kurudi Kwake tunapofanya kosa lile walilofanya la kuwa na miungu mingine, tumwombe aturudishe Kalvari. Je, tunabakije ndani Yake? Kwa kujifunza Biblia na kujiweka wakfu kwa ibada kila siku, tukiomba neema ya kuishi “kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu (Mathayo 4:4). Kwa kifupi, tumwamini na kumtii Yeye daima. Mungu atupe neema ya kufanya hivi. Ninawasihi vijana na watoto: “Chagueni hivi leo ni nani mtakayemtumikia.” Kuna ulazima wa kuazimia kuchagua sawa; kwa maana Yesu alisema, “Hamwezi kumumikia mabwana wawili, Mungu na mali. …” Ikiwa mioyo wetu imejaa upendo wa Kristo, itadhihirika kwamba Yeye ni Mwenye nguvu zaidi mioyoni mwetu kuliko tamaa ambazo zimetutawala, na anasa ambazo zimedhoofisha na kuleta misukumo mibaya, na kuiacha roho kwenye mtego wa majaribu ya Shetani…. Wakati moyo wa mwenye dhambi unaguswa, anayaachilia mapenzi yake kwenye mapenzi ya Mungu, naye anaona ndani ya Yesu kuvutiwa kusiko na kifani, na moyo wake unashawishiwa kumchagua Bwana.

Kushindwa kwa Israeli kutii kikamilifu amri za Mungu kwa kuwafukuza adui zao wote kulisababisha adui zao kuharibu upendo wa Israeli kwa Mungu kutoka ndani hadi nje. Yoshua alipokufa walionekana kama wanataka kumtafuta Mungu, ila walianza kumangamanga tena. Kutii baadhi ya amri za Mungu ni hatari, na ni sawa na kutozitii kabisa. Yote mawili yanaongoza kwenye uharibifu.

*Jina la Yesu Ndio Kiungo Kiunganishi Katika Maombi Kati ya Ubinadamu wote na MUNGU—Katika Jina la Kristo maombi yetu yanapanda juu kwa Baba. Yeye

hutuombea, na kututetea kwa niaba yetu na Baba anazianika wazi hazina zote za neema Yake kwa ajili ya kutumegea sisi, ili sisi tufurahie na kuwagawia wengine. “Ombeni kwa Jina Langu,” Kristo asema. Sisemi kwamba nitawaombea kwa Baba; kwa maana Baba Mwenyewe anawapenda ninyi. Litumieni Jina Langu mpate manufaa. Hii itayafanya maombi yenu yawe na ufanisi, na Baba atawapa utajiri wa neema Yake. Kwa hiyo ombeni, nanyi mtapata, ili furaha yenu iwe timilifu.”

---

Yoshua alikufa na miaka mingapi? Israeli walifanya dhambi gani? Kwa nini watu husahau matendo makuu ya Bwana? Unafikiri mwamuzi alikuwa na kazi gani? Kwa nini ni rahisi kurudi nyuma kiimani mambo yanapoenda kwa mafanikio?

**SIKU YA 61**
**(Machi 1)**

# Waamuzi wa Kwanza na Uasi wa Israeli - Waamuzi 3-6

Waamuzi walifanya kazi kama viongozi wa taifa wakiongozwa na Mungu. Israeli haikuwa na rais au mfalme, bali BWANA Mwenyewe alikuwa Ndiye mfalme wao. Kuna waamuzi 15 waliotajwa. Kuna mzunguko unaoonekana hauna mwisho katika Waamuzi: kumwacha Mungu, kuwa nyara za adui, kilio kwa Mungu cha kuomba msaada, ukombozi unaotolewa na Mungu, na kurudi katikanjia za ukaidi tena. Ubinafsi ulijirudia walipoacha kujali na kusimulia matendo makuu ya uaminifu wa Mungu! Musa na Yoshua walikuwa wamekufa. Kizazi hiki kilionekana kuwa na fursa kubwa, kwa vile walikuwa wamefika kwenye nchi ya ahadi iliyojaa maziwa na asali. Nao wakabweteka na wasiendelee kuwafukuza maadui. Vivyo hivyo nasi, tunaporuhusu maishani mwetu kile ambacho Mungu ametuamuru tukiharibu kabisa, kwa kukitokomeza, hicho kinatumika kama mwiba katika mbavu zetu. Tukimruhusu adui wa ubinafsi na sanamu kukua kwa nguvu hatimaye atatuangamiza. Ni "Baali" gani katika maisha yako ambaye unajaribiwa kumwabudu leo? Kutii kwa hofu siku zote husaidia kwa muda mfupi tu, bali utii unaochochewa na upendo ndio ambao unadumu. Tuuangalie msalaba kwa makini ili tupate kuwa na upendo kwa watu na Mungu. Yesu anasema, "Mkinipenda, mtazishika amri zangu." (Yohana 14:15 ).

Mwamuzi wa kwanza ni Othnieli aliyemwoa binti wa Kalebu aitwaye Aksa aliyewaamua Israeli kwa miaka 40. Na alipokufa Israeli ikafanya maovu mbele za BWANA, Naye akawatia katika mikono ya Moabu nao wakamtumikia mfalme wao. Walipomlilia BWANA Ambaye ana huruma nyingi, Bwana alimwunia mwamuzi aitwaye Ehudi wa kabila la Benjamini. Alipiga tarumbeta na kutangaza kuwa BWANA amewatia adui zao mikono mwao. Basi wakawapiga Wamoabu na Israeli ikawa na amani kwa muda wa miaka 80. Baada ya Ehudi, wana wa Israeli wakafanya maovu tena na Bwana akawatia katika mikono ya mfalme Yabini wa Kanaani na Sisera alikuwa amiri wa jeshi lake. Wana wa Israeli walipomlilia Mungu, alimwinua Debora, nabii mke awe mwamuzi, naye alikaa chini ya mtende wa Debora kati ya Rama na Betheli huko katika vilima vya Efraimu. Debora alimwita Baraka akamwambia aende kumpiga Sisera Naye Mungu atamtia mkononi mwake. Baraka akaogopa na akaomba "kwenda pamoja na Debora" akisema "kama huendi, pamoja nami, mimi siendi." Debora akamwambia ataenda ila heshima itaenda kwa mwanamke.

Basi Debora akaenda vitani na Baraka. Debora akamwambia Baraka "inuka maana siku hii ndiyo siku ambayo BWANA amemtia Sisera katika mkono wako, Je! BWANA hakutoka atangulie mbele yako?" BWANA akamfadhaisha Sisera na magari na jeshi lake lote mbele ya Baraka. Sisera akashuka kwenye magari yake ya chuma na kukimbia. Akafika mahali penye hema ambapo Yaeli alikuwepo. Yaeli alitoka kumlaki na kumkaribisha, kwamba asiogope. Aliomba maji ya kunywa kwani alikuwa na kiu

na akapewa maziwa na Yaeli. Sisera akaomba Yaeli asimame mlangoni mwa hema kumlinda, na yeyote ajaye akiulizia kuna mtu aseme hapana. Sisera alilala fofofo pengine kwa sababu ya kuchoka sana kwa vita na fadhaa. Hapo ndipo Yaeli alichukua kigingi cha mti akamwendea polepole asiamke na kukipigilia kwenye paji la uso la Sisera. Basi Baraka alipoendelea kumtafuta Sisera Yaeli alimwona na kumwita aje, alimwambia "njoo, nami nitakuonyesha yule mtu unayemtafuta." Akaona kigingi kipajini pa Sisera na hivyo Mungu akamshinda Yabini mfalme wa Kanaani. Debora na Baraka waliimba wimbo wa ushindi wakimtumkuza Mungu kwa kuondoa adui zao.

Debora akawaamua Israeli miaka 40. Wana wa Israeli wakafanya maovu tena, na Bwana akawatia mikononi mwa Wamidiani. Waisraeli walienda chini kwenye kuabudu miungu mingine na maovu, na walipotiwa utumwani na kupata mateso walimrudia Mungu na wakapata mwamuzi. Kisha wakasahau tena kuwa nuru kwa mataifa, na kisa kikajirudia tena na tena.

Je, wewe ni dhaifu leo? Je, kutotii kwako mwenyewe kumeuponda moyo wako? Usivunjike moyo. Sio tu kwamba Mungu huwaadibu wale Anaowapenda, lakini anafurahia kuwaweka huru. Je, utampa Mungu udhaifu wako? Ana mipango sio tu ya kukutoa wewe, bali pia kukuwezesha kuwakomboa wengine.
Kisa cha Israel ni kisa chetu, na Mungu wa Israel pia ni Mungu wetu, kwani tunapomwita Yeye hutusikia na anakuja kukuokoa. Je, unaweza kushuhudia hili maishani mwako?

Yohana anatoa muhtasari akisema "Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. 1Yohana 2:16 . Hebu tuelewe wazi na kwa uhalisi mahali petu ulimwenguni: tumezaliwa na hatia, Mungu anajua hilo, na Yeye hatuvizii ili atukamate na hatia bali anatafuta njia ya kutuokoa. Tusipoishi kwa Neno la Mungu, tunakaribisha msiba/ole. Je, wewe ni dhaifu leo? Je, kutotii kwako mwenyewe kumekuponda moyo? Usivunjike moyo. Sio tu Mungu huwaadhibu wale anaowapenda, lakini pia anafurahia kuwaweka huru. Je, utampa Mungu udhaifu wako? Yeye Ana mipango ya kukutoa wewe kwenye shimo na, pia kukuwezesha uwakomboe wengine.
Sisi kama waisraeli mara nyingi ni lazima tupitie shida ili tuweze kuvutwa na kumrudia Mungu. Hicho ndicho kisa cha mwana mpotevu. Tunapowaombea waliopotea, Mungu hufanya yote anayoweza kufanya ili kuwarejesha watoto Wake, lakini sisi tuko huru kukataa mwito Wake. Kupuuza jumbe ambazo Mungu anaona ni muhimu kwa watu Wake katika siku za mwisho ni kujimaliza wenyewe. Kwa hiyo agizo la Biblia linalosema, "Nisikieni, enyi Yuda nanyi wenyeji wa Yerusalemu: Mwaminini Bwana Mungu wenu, nanyi mtathibitika; waaminini manabii Wake, nanyi mtafanikiwa" ni la kweli kabisa

Ijapokuwa tunapaswa kuimba yale ambayo Mungu ametufanyia zamani, tunapaswa pia kuimba wimbo mpya wa yale ambayo Mungu ametufanyia sasa. Mara nyingi sana katika maisha yangu, nashindwa kuyaandika, nashindwa kuyaona matendo makuu ya Mungu katika maisha yangu yanayoendelea kwa sasa. Na ninapokosa kukumbuka jinsi Mungu ananiongoza katika maisha yangu leo, huwa ninaanza

kuhofia wakati ujao. Na tumwimbie Bwana wimbo mpya, wimbo wetu kibinafsi wenye uzoefu wa kina, wa jinsi Mungu anavyofanya kazi katika maisha yetu leo. Hata Mungu pia anaimba juu yetu. “Bwana, Mungu wako, Yu katikati yako shujaa awezaye kuokoa; Atakushangilia kwa furaha kuu, Atakutuliza katika upendo Wake, Atakufurahia kwa kuimba” Sefania 3:17. Mungu wa vita aliwapigania Israeli, haukuwa ujuzi wao katika vita, wala wingi wa hesabu yao, au silaha.

*Ndio, Kristo amekuwa njia ya maombi kati ya mwanadamu na MUNGU (kiwambaza cha kati). Pia amekuwa njia ya baraka kati ya MUNGU na mwanadamu. Ameunganisha Uungu na ubinadamu. Watu wanapaswa kushirikiana Naye kwa ajili ya wokovu wa roho zao wenyewe, na kisha kufanya bidii, na jitihada za dhati zenye kudumu ili kuokoa wale ambao wako tayari kufa hatarini.

---

Jina la mwamuzi wa kwanza ni nani? Mwamuzi wa pili alitawala kwa miaka mingapi? Je, tunawezaje kulinganisha kati ya mwamuzi na rais wa nchi? Yaeli alikuwa nani? Debora aliamua kwa miaka mingapi? Kwa nini Sisera alishuka kwenye gari la chuma? Kitu gani tusipokikiacha au kukiteketeza kitatuharibia mambo?

**SIKU YA 62**
**(Machi 2)**

# Gideoni- Je, uko Tayari Kuondoa vitu 31,700 Kwenye Maisha Yako

**- Waamuzi 6-9**

Baada ya miaka saba chini ya kongwa la Wamidiani, mambo yalikuwa mabaya sana mpaka watu wakatoroka nyumba zao na kuishi kwenye mapango, au mashimo. Waisraeli walipolima mashamba Wamidiani na Waamaleki wakakwea na kuharibu mazao yao na kuchukua mifugo yao, iwe kondoo, punda, au ng'ombe. Waliingia kwenye nchi yao na kuiharibu. Israeli ikatwezwa sana na Wamidiani, nao wakamlilia BWANA. BWANA akamtuma nabii kuwaambia Yeye Ndiye BWANA Mungu aliyewatoa Israeli katika utumwa. Malaika wa BWANA akaketi chini ya Mwaloni wa Ofra ambapo kijana Gideoni au Yerubaali alikuwa akipepeta ngano ili aifiche machoni pa Wamidiani. Akasikia Malaika akisema "BWANA yu pamoja nawe ewe shujaa." Gideoni akamjibu kuwa kama BWANA yu pamoja naye inakuwaje basi mambo haya ya utumwa yamewapata. Akauliza, "yako wapi matendo yake ya ajabu, waliyotuhadithia babu zetu?" BWANA akamtazama na kumwambia aende kwa uwezo Wake na awaokoe Israeli na mkono wa Wamidiani. "Je si Mimi niliyekutuma." Gideoni japo alinenwa kuwa ni shujaa, alikuwa ni mwoga naye akatoa udhuru kwamba atawaokoa Waisraeli kwa jinsi gani na kabila lake ndilo maskini naye ndiye mdogo katika nyumba ya baba yake. Malaika wa BWANA alimhakikishia kwamba atakuwa pamoja naye, naye Gideoni atawapiga Wamidiani kama mtu mmoja. Vita ni vya Mungu! Unakabiliwa na vita gani leo? Ni adui gani amekusanya nguvu dhidi yako? Angalia juu rafiki yangu. Mpaji wako msaada katika shida ni Bwana!Vita sio vyetu. Vita ni vya BWANA , Naye atatuokoa. Tunapenda kuhesabu namba, tuna walimu wangapi? Wachungaji wangapi? wazee wangapi? Tuna pesa kiasi gani kwenye salio la akaunti yetu ya benki? Kuna chakula cha kutosha? kuna watu wa kujitolea wa kutosha? kutaniko letu si kubwa vya kutosha nk. Tunaweka imani yetu kwenye idadi na rasilimali kama vile Gideoni au Filipo (wakati wa kulisha 5000). binadamu huona



kuwa kuna nguvu katika idadi. Ila Si kwa idadi, bali kwa uwezo wa Mungu kwamba kazi itakamilika. Sote tuchague kwa dhati kuwa miongoni mwa wachache ambao Mungu atawatumia.

Gideoni akamwambia malaika ampe ishara kama amepata "kibali mbele ya macho yako." Akamsihi asiondoke mpaka atoe sadaka yake, basi aliendа ndani na kutoa mbuzi na mkate usiyotiwa chachu na unga, kisha akatia mchuzi na kuuleta kwa malaika. Malaika wa BWANA alinyosha ncha ya fimbo kwenye sadaka na moto ukatoka mwambani na kuiteketeza ile sadaka, na malaika akaondoka mbele zake

Gideoni alijua ni Malaika wa BWANA na aliogopa kwamba huenda atakufa. asiogope "hatakufa." Gideoni akamjengea BWANA madhabahu. Usiku huo BWANA alimwambia aangushe madhabahu ya Baali na kutoa sadaka ya ng'ombe. Gideoni aliwaogopa watu wa nyumba ya baba yake maana babaye alikuwa na miungu. Pia Aliwaogopa watu wa mji na hivyo alifanya haya usiku na watu walipoamka asubuhi waliona madhabahu ya Baali imebomolewa, na ng'ombe ametolewa sadaka. Wakaulizana "Ni nani ametenda haya?"

Basi Wamidiani waliingia bondeni kuwafuata ila Roho ya BWANA ikaja juu ya Gideoni naye akapiga tarumbeta ya watu kukutanika. Naye akamwambia Mungu, kuwa kama atawaokoa Israeli kama alivyosema, "nitaweka ngozi ya kondoo katika kiwanja na kama ukiwapo umande juu ya ngozi tu na nchi yote ni kavu, ndipo nitajua kwamba utawaokoa waisraeli." Basi alipokuja asubuhi alikuta maji na akakamua bakuli zima la maji kutoka kwa ile ngozi. Gideoni akamwambia Mungu "hasira Yako isiwake juu yangu" akaomba ishara nyingine ya mwisho! Akisema "sasa ngozi tu na iwe kavu mara hii tu" na umande uwe juu ya nchi yote. Alipoamka asubuhi alikuta umande juu ya nchi yote bali ngozi ilikuwa kavu.

Watu walianza kuja kwa Gideoni mpaka wakafika 32,000. Gideoni akawafuata wale Wamidiani na jeshi lake, lakini BWANA akamwambia, watu hawa ni wengi mno. Jeshi la watu hawa lilikuwa na hatari ya kiburi na kufikiri kuwa wameshinda kwa nguvu zao. Mungu hashindi kwaajili ya namba! Basi akawaambia wale wote wanaoogopa na kutetemeka warudi majumbani mwao. Ndipo watu 22,000 wakarudi na wakabaki 10,000 tu. Bila shaka Gideoni alishangaa kuona maaskari wengi wakirejea nyuma. BWANA akamwambia kuwa atachuja tena ili wapungue. Basi akawaleta kwenye maji na kumwambia Gideoni kuwa yule aliyeramba maji kwa ulimi kama vile mbwa akipeleka kinywani" mchukue, bali yule aliyepiga magoti kunywa, mwache. Basi wakabaki watu mia tatu baada ya mchujo huu. Mungu akawatia Wamidiani kwenye mikono ya jeshi la Gideoni. Wale watu 300 walipangwa kwenye vikosi vitatu na tarumbeta na mitungi isiyo na maji na mienge ndani ya mitungi. Walipiga tarumbeta na kuvunja mitungi na kushika mienge. Basi BWANA akaufanya upanga wa Wamidiani uwe kila mmoja juu ya mwenzie na juu ya jeshi lote, wakakimbia. Watu wa Israeli wakamwambia Gideoni awe mtawala wao au mwamuzi. Lakini akasema mimi sitatawala wala mtoto wangu au mjukuu bali BWANA. Nchi ilipata amani kwa miaka 40.

Wakati mwingine mateso husababishwa na maamuzi ya dhambi. Wakati mwingine husababishwa na ulimwengu wenye dhambi, uliovunjika. Na wakati mwingine hakuna sababu inayotambulika. Je, unataka kujua "kwa nini" mateso na maumivu ya moyo yapo humu duniani? Kwa kweli binadamu mara nyingi hana maelezo kamili. Siku moja Bwana atatueleza kinagaubaga. Pengine swali la muhimu zaidi kwetu ni "Ninawezaje kukua kupitia mateso haya?" Uchunguzi huo unageuza mateso kuwa hazina. Siku moja, tutajua sababu sababishi. Ila siyo sasa! Kinachoonekana wazi katika sura hii ni kwamba Mungu hawaiti walio na nguvu au waliohitimu zaidi, bali anawaita wale ambao watamletea utukufu. Tunaweza kuona kwamba hakuna kitu ndani yetu, ila tujikabidhi Kwake, Yeye atatuelekeza. Tunahitaji upole, uvumilivu na utu wema lakini pia tu nahitaji kuwa na ujasiri! Ijapokuwa kila mara watu hawa walijiletea taabu wenyewe kwa kutenda maovu, Mungu aliwajibu kwa wema kilio chao cha ukombozi. Mungu ni Mwenye neema na rehema. Hii inaleta matumaini kwetu. Maisha yanaendelea kuwa mabaya kwenye sayari hii. Basi tumlilie BWANA atukomboe. Tunachohitaji sasa ni nguvu ya mvua ya masika ya Roho Mtakatifu ili kumaliza kazi ya injili. Kazi itakapokamilika, Yesu atakuja.

Hebu tuombe basi kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu. Baba yetu wa mbinguni Yuko tayari zaidi kuwapa Roho Wake Mtakatifu wale wanaomwomba, kuliko wazazi wa duniani wanavyotamani kuwapa watoto wao zawadi nzuri. Lakini ni kazi yetu, kuungama, kujidhili, kutubu, na kwa maombi ya dhati, kutimiza masharti ambayo kwayo Mungu ameahidi kutupa baraka Zake. Uamsho huletwa kwa kujibu maombi yetu. Tumepokezwa kijiti ambacho inabidi tukimbie nacho katika kufanya matengenezo!

*Bado wanafunzi walikuwa hawajui rasilimali na nguvu za Mwokozi zisizo na kikomo. Akawaambia, "Mpaka sasa hamkuomba chochote kwa Jina Langu." Yohana 16:24. Alielezea kuwa siri ya mafanikio yao itakuwa katika kuomba nguvu na neema kwa Jina Lake. Kwamba Yeye Atakuwepo mbele za Baba kuwaombea. Maombi ya mwombaji mnyenyekevu huwasilishwa Naye kama matamanio Yake Mwenyewe kwa niaba ya roho hiyo. Kila ombi la dhati husikika mbinguni. Linaweza lisiwasilishwe kwa ufasaha/umbuji; lakini ikiwa linatoka moyoni, litapanda kwenda mahali Patakatifu ambapo Yesu anahudumu, na ataliwasilisha kwa Baba bila hata Neno moja lisilopendeza, lenye kuudhi, gumu au lenye kigugumizi, bali kwa Neno zuri na lenye harufu nzuri ya ubani wa ukamilifu Wake Mwenyewe.

---

Malaika alimtokeaje Gideoni? Gideoni aliomba ishara gani tatu? Jeshi lilipunguaje mpaka kuwa 300? Hiyo ni asilimia ngapi ya 32,000? Kwa nini Gideoni aliogopa watu wa nyumba ya baba yake?

**SIKU YA 63**
**(Machi 4)**

# Yeftha na Nadhiri ya Kafara

**- Waamuzi 9-13**

Gideoni alikuwa na hekima na hakupenda kugombana. Watu wa Efraimu walipomjia na kusema mbona hakuwaita kupigana na Wamidiani? Alijibu kwamba wao wamefanya machache kulinganisha na Waefraimu, na mavuno yao ni mema na wameshasaidia kuwapiga wafalme wawili wa Midiani. Alisema, "mimi nimefanya nini sasa kama mlivyofanya ninyi?", na Waefraimu wakatuliza hasira zao.

Mara nyingi mtu anapofanya jambo kubwa, watu humtaka awe kiongozi wao kama ilivyokuwa kwa Gideoni. Tunawainua wanaume na wanawake ambao wamefanya mambo makubwa tukitarajia zaidi kutoka kwao. Hili linawapa majaribu na kupunguza kasi ya maendeleo ambayo Mungu anataka kuyaona katika maisha yao na yetu wenyewe. Je, tumesababisha majaribu makubwa zaidi kuwashabikia wachungaji au viongozi ili wasingoe viburi na tumefanya 'vichwa vyao kuvimba'. Kwa nini tunapata ugumu sana kumfanya Mungu kuwa kiongozi wetu? Yeye ameonyesha tena na tena uaminifu Wake, uongozi Wake, na kujitolea Kwake katika kutimiza agano. Basi sote tuendelee kuwainua viongozi wetu katika sala, ili wawe watumishi wanyenyekevu kwa Mungu. Bwana asamehe kiongozi yeyote kati yetu aliye na kiburi kinachomharibia ushuhuda wake wa wema wa Mungu, na atuongoze kwenye toba na kugeuka kutoka kwa dhambi kama hizo. Muda ni mfupi ndugu zangu, maisha yetu yawe kielelezo cha furaha ya wokovu wetu katika Kristo Yesu.

Gideoni aliepuka vita vya wenyewe kwa wenyewe na Waisraeli wenzake, kwa jinsi alivyowajibu Waefraimu (Waamuzi 8:2-3). Kiini cha kile alichosema ni kwamba kile alichokuwa ametimiza hakikuwa chochote ikilinganishwa na kile walichokipata katika kuwaua makamanda wawili wa jeshi la Wamedi—Orebu na Zeebu . "Kisha hasira yao kwake ikapungua aliposema hivyo." Biblia inasema, "Jawabu la upole hugeuza hasira, bali neno liumizalo huchochea hasira." Mithali 15:1. Je, watu wangezuia malumbano au talaka ikiwa kungekuwa na jibu laini kutoka kwa kijana, mtoto, mume au mke? Je, mgogoro unaoendelea kati ya marafiki wawili wa zamani ungeweza kuepukwa ikiwa kungekuwa na jibu laini kutoka kwa mmoja wao? Si rahisi kutoa jibu laini kwa mtu ambaye anakushtaki kwa jeuri kwa yale ambayo hujayafanya. Hilo hufanya kutokeza kwa ujeuri wetu wenyewe, na kisha tukajibu vivyo hivyo, na mlipuko unatokea. Lakini tukiomba kwa ajili ya neema ya kutoa jibu laini kama Gideoni alivyofanya, mzozo unaepukika. Wakati mwingine unapoudhika, omba neema ya kutuliza mvutano kwa kutoa jibu laini. "Huwezi kubadilisha jinsi watu wanavyokuchukulia au kile wanachosema kukuhusu. Unachoweza kufanya ni kubadili jinsi unavyoitikia." Kwa neema ya Mungu - na neema ya Mungu pekee—tunaweza kuguswa vyema na kichocheo hasi nasi tusilipuke! Maneno ya Kinywa changu na mawazo ya moyo wangu yaweze kukubalika Kwako, Eh Mungu

Mwamba wangu na Wokovu wangu, ndiyo ombi langu leo.

Ingawa Gideoni alikuwa na dhambi ya kutengeneza naivera inayovutia ibada ya sanamu kwa Israeli na alikuwa na masuriakadhaa katika miaka ya mwisho wa maisha yake, Mungu anatumia ubinadamu uliovunjika kufikia kusudi Lake na utukufu. Hiki si kisingizio cha kufanya dhambi, kwani Mungu anataka kutuokoa kutoka kwa dhambi zetu na kujenga mahusiano nasi hatua kwa hatua na hivyo kutusaidia kutafuta haki yake yote katika mchakato wa utakaso.



Alipokufa Gideoni wana Israeli wakakengeuka na kuasi, wakiabudu miungu mingine kama Baali. Hawakumkumbuka Mungu aliyewaokoa dhidi ya adui zao pande zote. Basi Abimeleki alipokuwa mwamuzi, aliajiri watu wapuuzi na mabaradhuli wafuatane naye. Kisha aliwaua ndugu zake wote kwa mashauri mabaya na kutaka atawale. Huu ni uovu na dhambi. Yothamu aliye mdogo alisaidiwa akajificha akimwogopa nduguye Abimeleki. Abimeleki, alikufa kwa kubwagiwa jiwe la kusagia kichwani toka juu ya nyumba. Hivyo ndivyo Mungu alivyolipiza kisasi juu ya uovu aliotenda Abimeleki na watu wa Shekemu wa kuwaua ndugu zake 70. Kutamani makuu ni jambo la hatari sana kwani ni hekima nzuri kubaki na malengo ya kumheshimu Mungu dhidi ya kujiridhisha. Mtu anaweza kujitafutia nafasi si kwaajili ya kutoa huduma, lakini kutaka kuwa dikteta au kuhamia mahali ambapo pesa zaidi zinaweza kupatikana. Yabidi kuelewa maandiko na kuyatenda, kumwelewa Mungu, na kuelewa maana ya kuwa muumini anayekwenda mbinguni. Mmoja wa Waamuzi alikuwa ni Yeftha. Waamoni walipowakabili Israeli, Israeli walimwita Yeftha aende kuwasaidia naye akasema mbona mlinichukia na kunifukuza nitoke katika nyumba ya baba yangu? Wakamwambia sasa wamegeuka na kuwa wazuri, na wakamwambia, "wewe utakuwa kichwa chetu." Yeftha alienda pamoja na wazee hao na akawa kiongozi wao. "Yeftha akanena maneno yake yote mbele ya BWANA huko Mispa." Basi akatuma ujumbe kwa mfalme wa Waamoni akimwuliza kwa nini wanaleta uchokozi; naye akajibu kwamba Israeli walitwaa nchi yake walipotoka Misri. Naye Yeftha akaeleza namna Mungu alivyowasaidia kupata nchi hiyo. "Je, wewe u mwema kuliko Balaki mwana wa Sipori…Je, yeye alishindana na Israeli, au kupigana nao?" Mwishowe akasema, "mimi sikukufanyia wewe dhambi lakini wewe umenitenda uovu kwa kupigana nami." Akasema BWANA awe mwamuzi kati ya Israeli na Waamoni, lakini mfalme hakusikiliza maneno ya Yeftha. Roho ya BWANA

ikamjia Yeftha naye kabla hajaenda kupigana aliweka nadhiri, akisema endapo Mungu atawatia Waamoni mikononi mwake, itakuwa, "kile kitakachotoka katika milango ya nyumba yangu kunilaki, hapo nitakaporudi na amani kutoka kwa hao wana wa Amoni, kitu hicho kitakuwa ni cha BWANA, nami nitakisongeza kiwe sadaka ya kuteketezwa." Mungu hataki sadaka za kuteketezwa za wanadamu. Ila Yeftha katika mtanziko wake alijikuta amesema hili bila kufikiri. Yeftha alikuwa na mtoto mmoja tu na alimpenda mno, na binti alimpenda baba.

Kila mtu duniani amezaliwa ili kumpa Mungu utukufu kwa kutekekeliza utume fulani wa pekee ambao hakuna mwingine anaweza kuufanya. Kama wale walio karibu yako au kwenye uongozi hawakubaliani na kile Mungu amekuita kukifanya, wahitaji kuendelea kuombea jambo hilo. Wengi hutumia uzoefu, mapokeo au akili za mwanadamu wanapoipima kazi waliyopewa na Mungu au ile watu wengine waliyopewa na Mungu, na hivyo wanaweza kuingiza mambo hasi ambayo yanaweza kukukatisha tamaa. Kama utafanya kazi na watu ambao hawakuelewi, au hawatambui kile kilicho ndani yako, hao watakuwa na mashaka na wewe. Ila siyo lazima ushikamane nao sana (best friend). Ikiwa Mungu amekutuma, atakuletea watu watakaokuelewa nao watakusaidia kusonga mbele. Daima baada ya kujua kile Mungu anataka ufanye kwa maombi na kusoma Maandiko songa mbele. Wale wasiokulewa kawaida hawakai nyadhifa hizo milele, wanaweza wakahamishwa au wakastaafu. Watakapoondoka, utapata watu wengine wa kukuunga mkono. Kikubwa ni kujiweka wakfu kwa Bwana, na usimtendee Mungu dhambi, maana ukifanya hivyo utapata watu wengi wa kukuzomea, na kuizomea kazi ya Mungu. Na mara zingine watu waliokupinga wakimwagiwa Roho Mtakatifu, watarudi na kukwambia kwamba pale walikosea. Lakini hata wasiporudi, wewe songa mbele, kwa ujasiri, unyenyekevu, na bila malumbano, ukishirikisha wengine kadri iwezekanavyo.

Yeftha aliend kupigana na Waamoni na Waamoni wakashindwa mbele ya Waisraeli. Akafika Mispa nyumbani mwake, akiwa ametoka vitani na tazama binti yake ndiye aliyekuja kumlaki na matari na machezo, naye alikuwa mwanawe wa pekee. Alipomwona binti yake akararua mavazi yake, akasema "ole wangu! mwanangu umenitweza sana, nawe u mmoja miongoni mwa hao wanisumbuao; kwa kuwa mimi nimemfunulia BWANA kinywa changu, nami siwezi kurejea nyuma." Kweli ilimpa baba uchungu; binti anaimba kwa furaha na matari, bali baba ana huzuni kubwa. Basi binti alimwambia baba yake endapo alifunua kinywa chake kwa BWANA na kumpa nadhiri, "basi unifanyie sawa sawa na hayo yaliyokutoka kinywani mwako kwa kuwa Yeye ni BWANA," maana amewalipa adui zako kisasi. Basi binti yule alimwambia baba yake amruhusu aende milimani na kuomboleza ujana wake na wenzake. Baba yake akamwambia aende yeye na wenziwe kuomboleza uanawali wake. Mwisho wa miezi miwili alirudi na baba yake alitimiza nadhiri aliyotoa. Tunaona hata Waamoni walimchukiza Mungu wakitoa kafara ya kuteketeza ya watoto wao kwa mungu wao aitwaye moleki, Mungu haitaji kafara ya binadamu ya namna hiyo. Kafara inayohitajika kuitoa ni talanta, maisha, fedha, mvuto, moyo uliopondeka, au muda wetu kusaidia wokovu wetu na wa wengine. Hatuwezi kusema Yeftha alitaka kufanya kama Waamoni. Hili ndilo mojawapo ya mambo tutauliza tukifika mbinguni ili tuelewe vizuri; hivyo watoto tujitahidi kufika pale. Hata hivyo cha kujifunza hapa, ni kumwomba Mungu ili atuongoze tunapoweka nadhiri. Maana

tufanyapo nadhiri kwa Mungu ni lazima tutimize. Yeye hatuombi tutoe nadhiri bali ni sisi ndio wakati mwingine tunasema kwa haraka bila kufikiri na kisha tunajuta ni kwa nini tumesema kwa haraka vile? Yeftha alikuwa mwamuzi kwa miaka sita akafa, kisha walifuata waamuzi wengine. Na habari hii ikajirudia tena na tena mwamuzi alipokufa. “Wana wa Israeli wakafanya yaliyo mabaya mbele ya macho ya Bwana. Bwana akawatia katika mikono ya Wafilisti.”

*Wanafunzi walipaswa kuendeleza kazi yao katika Jina la Kristo. Kila neno na tendo lao lilipaswa kukazia fikira juu ya Jina Lake, kama lililo na nguvu muhimu ambayo kwayo wenye dhambi wanaweza kuokolewa. Imani yao ilikuwa ni kujikita ndani yake ambaye ni chanzo cha rehema na nguvu. Katika jina Lake walipaswa kuwasilisha maombi yao kwa Baba, na walipokea majibu. Walipaswa kubatiza kwa jina la Baba, la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Jina la Kristo lilipaswa kuwa ulinzi wao, kitambulisho cha utofauti wao, kifungo chao cha muungano, mamlaka ya mwenendo wao, na chanzo cha mafanikio yao.

---

Ni nani alikuwa mwamuzi baada ya Gideoni? Je, ni mambo gani Gideoni alifanya vizuri na yapi alifanya vibaya? Kwa nini nadhiri ya Yeftha ilikuwa si ya kawaida? Ni nini kilichomfanya aifanye?

**SIKU YA 64**
**(Machi 5)**

# Samsoni Mnadhiri wa Mungu Aliyewa na Maguvu Kupita Binadamu yoyote

**- Waamuzi 13 na 14**

Basi wana wa Israeli walipofanya maovu machoni pa BWANA, aliwatia mikononi mwa Wafilisti kwa muda wa miaka 40. Palikuwa na mtu mmoja aliyeitwa Manoa, na mkewe alikuwa tasa, hakuzaa mtoto. Malaika wa BWANA akamtokea huyu mwanamke na kumwambia kuwa atachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume na wembe usipite juu ya kichwa chake maana mtoto huyu atakuwa mnadhiri wa Mungu tangu tumboni naye ataanza kuwaokoa Israeli dhidi ya Wafilisti. Somo hili linaonesha kuwa chakula tunachokula ni muhimu kwa maisha ya kiroho na kimwili pia. Mke wa Manoa akaenda na kumwambia mume wake, "Mtu wa Mungu alinijia," uso wake ulikuwa kama Malaika wa Mungu na wa kutisha sana, ila sikumwuliza ametoka wapi.

Akaendelea kueleza ujumbe aliosema kuwa atachukua mimba na kuzaa mwana wa kiume. Mtoto huyo asinywe divai wala kileo wala kitu kilicho najisi, maana mtoto huyu atakuwa mnadhiri wa Mungu toka tumboni hata siku ya kufa kwake. Ndipo mume wake akamwomba Bwana kwamba mtu aliyemtokea mke wake aje tena na kuwafundisha yawapasayo kumfanyia huyo mtoto atakayezaliwa. Ni muhimu sana kwa wazazi kujua jinsi Mungu anavyotaka tutunze watoto wetu. Biblia ndiyo kitabu cha kwanza kwa uzuri na uhakika kwa malezi ya mtoto. Tusitunze watoto kwa kubahatisha, au kutokana na destruri za watu wa dunia. BWANA aliisikiliza sauti ya Manoa na malaika wa Mungu akamtokea tena mke wake mara ya pili akiwa shambani peke yake. Bahati kubwa hii, kupata maagizo ya jinsi ya kulea mtoto kwa mara ya pili. Mama huyu akapiga mbio kumwita mume wake na kumwambia afuatane naye maana "yule mtu aliyenitokea amerudi tena." Basi Manoa akaenda na mke wake na alipofika kwa huyu mtu alimwuliza kama ndiye yeye aliyezungumza na mke wake hapo kwanza, akasema "Naam ni mimi. Manoa akasema hayo maneno yatakapotimia, Je! Huyo mtoto atakuwa wa namna gani, na kazi yake itakuwa nini? Malaika wa Mungu akamwambia ile miiko yote aliyomwambia mkewe, na kusisitiza waishike. Manoa alimwomba malaika angoje ili wamchinjie mwana mbuzi lakini malaika akasema kuwa japo amemsihi hatangoja na wakati wa kutoa kafara ukifika, basi amtolee BWANA. Malaika ni watumishi wa Mungu, hivyo wanakataa kusujudiwa na kuchukua utukufu ambao ni Mungu tu anastahili. Kila mtu ana Malaika wake. Manoa hakujua kuwa huyu ni Malaika, akamwuliza jina lake na Malaika akasema kwani wewe kuniuliza jina langu ni la ajabu wewe kuelewa.

Hata leo wapo wazazi wanaouliza hilo swali, yaani, tutamleaje mtoto! Manoa alikuwa na ombi zuri. Manoa alitoa kafara ya mwana mbuzi pamoja na sadaka ya unga kwa BWANA juu ya mwamba, na yule Malaika akatenda jambo la

ajabu wakiangalia, kwani mwali wa moto ulipopaa mbinguni toka madhabahuni na Malaika Naye akapaa katika mwali wa moto, manoa na mkewe wakaanguka kifudifudi na kusujudu. Malaika huyu hakurudi tena kwao, na Manoa akamwambia mke wake kwamba watakufa kwa sababu wamemwona Mungu. Mkewe kwa hekima akasema, kama Mungu angetaka kuwaua kwa nini amewaonesha haya yote na sadaka yao ikapokelewa, hata hivyo asingewaambia kama watapata mtoto kama watakufa. Mke wa Manoa alizaa mwana akamwita jina lake Samsoni, naye akakua, na BWANA akambariki na Roho ya BWANA ikaanza kuwaka ndani yake. Manoa na mkewe walifanya kazi njema kumtunza mtoto wao. Hata hivyo Samsoni hakuwa mwaminifu. Baada ya kukua, akatelemkia mji wa Timna, amfuate binti wa Wafilisti, naye akawaambia wazazi wake kwamba wampatie huyo amwoe. Tunapogundua udhaifu wetu, hebu tumlilie Mungu ili atupatie nguvu za kushinda dhambi zinazotuzinga kwa wepesi. Basi baba na mama ya Samsoni walimwuliza, je, hapana mwanamke wa kabila au jamaa zetu mpaka uende kuoa kwa Wafilisti wasiomwabudu Mungu wa mbinguni? Naye akasema "mnipatie huyo, kwa maana ananipendeza sana." Inaonekana Samsoni alikuwa na misukumo ya rika, na mapenzi yasiyofaa yaani uasherati. Mtu akitaka kuoa, asiangalie mapenzi yake tu, bali Mapenzi ya Mungu kwanza. Watu wengi hujiingiza katika shida kwa kuoa mtu ambaye hamwamini Mungu maana na watu usema mahapa yana upofu, ila upendo wa kweli hauna upofu. Wakati huu Wafilisti walikuwa wakitawala Israeli na pengine BWANA alitumia njia hii kutaka kisa juu ya Wafilisti. Samsoni na wazazi wake walitelemka Timna kwenye mashamba ya zabibu na mwana simba akaunguruma. Roho ya BWANA ikamjia kwa nguvu naye akapasua mwana simba kama mbuzi bila chombo chochote mikononi. Inaonekana shamba lilikuwa kubwa na hawakuona jinsi Samsoni alivyomwua simba. Alitelemka na kuzungumza na huyo mwanamke tena siku nyingine na akapendezwa Naye zaidi. Jambo ambalo ni dhambi kuoa mtu asiyemwamini Mungu. Alipopita pale kwenye mzoga wa simba aliona nyuki wengi kwenye mzoga na asali ilikuwepo. Aliwapa baba na mama yake asali, bila kusema ameitoa wapi.

Hapa kuna changamoto kubwa kwani Biblia inasema kwamba hatupaswi kufungiwa nira na wale wasioamini. Hii ina maana kwa washiriki na viongozi wa Kiroho kama Samsoni. Ila kuna watu wanakutana na kisha mwingine anaamini baada ya ndoa, au kuna wengine wanaacha imani baada ya ndoa. Hapo kutokana na mashauri ya Paulo, mtu huyo asimwache mume au mke wake. Kwani sote tutahukumiwa kwa kanuni takatifu ya Mungu, Mungu anasamehe kutojua ila tunapoelewa tunawajibika kabisa. Kabla ya ndoa ni vyema kujua kama yule mwenzi wako yuko tayari kufuata maagizo yote ya Bwana, yanayopatikana kwenye Maandiko Matakatifu. Maagizo ya Mungu yanalenga uaminifu Kwake na sio kuharibu nyumba na familia. Mungu amesema tusiwe na mahusiano na dunia kwa njia ambayo haimtukuzi. Umoja wetu na ulimwengu kwa mazoea, mtindo wa maisha, malengo au ndoto zetu, mara nyingi hutuweka mbali na Mungu. Watu wengine wameuliza waliposoma kitabu cha Ezra wakisema, Je, tunaweza leo kumtaliki mke asiyeamini kama ilivyotokea katika Ezra 10? Bwana wetu Yesu anatoa jibu:

"Mafarisayo nao wakamwendea, wakamjaribu na kumwambia, Je! ni halali mtu kumpa talaka mkewe kwa sababu yoyote tu? Akajibu, akawaambia, Hamkusoma

ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mume na mke, akasema, Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe, na hao wawili watakuwa mwili mmoja? Kwa hiyo, wao si wawili tena bali mwili mmoja. Kwa hiyo aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe."Wakamwambia, Mbona basi Musa aliamuru kumpa cheti cha talaka, na kumwacha? 'Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu, lakini tangu mwanzo haikuwa hivyo. Nami nawaambia ninyi, Kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa kwa sababu ya uasherati, na kuoa mwingine, azini; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini" (Mathayo 19:3-9). Kwa hiyo tuwatie moyo vijana wenzetu kusali kabla ya kuingia kwenye ndoa ili wasifanye makosa maana wakishaingia hakuna kutoka ila kwa sababu ile Yesu ametoa. Hivyo "Chunga kabla ya kuruka," ndiyo sera ya kufuata. Soma zaidi kwenye (1 Wakorintho 7:12-16 ).

Mambo yanaweza kuonekana magumu na mawimbi yanaweza kuwa makali katika kuchagua wa kuoa, ila , tumeitwa kung'oa mwelekeo wa mazoea au tabia yoyote ambayo hutuweka mbali na Mungu, na kufanya kinyume chake.Ombi: Bwana mpendwa, nisaidie kuwa mwaminifu kabisa kwa Neno Lako kwa sababu najua kwamba "katika mambo yote Wewe Bwana Mungu hufanya kazi pamoja na wale wakupendao katika kuwapatia mema, ambao umeweaita kwa kusudi Lako. ( Warumi 8:28 )

*Pale Patakatifu pa Patakatifu pana sanduku; juu na pande zake kuna dhahabu safi. Kila mwisho wa sanduku kuna kerubi mwenye kupendeza, na mabawa yake yametandazwa juu yake. Nyuso za makerubi wawili zinaelekeana, nao hutazama chini. Kati ya malaika hao kuna na chetezo cha dhahabu. Juu ya sanduku, pale waliposimama malaika, pana utukufu ung'aao sana, ukionekana kama kiti cha enzi alipokaa MUNGU. Yesu anasimama kipindi hiki kando ya sanduku, na sala za watakatifu zinapomjia, uvumba ndani ya chetezo nkatoka moshi, na Yeye anatoa sala zao pamoja na moshi wa uvumba kwa Baba Yake.

---

Baba yake Samsoni aliitwa nani? Malaika alimtokeaje mama yake Samsoni? Je, ni vyema kuoa mke au kuolewa na mtu kwa sababu unapendezwa naye tu, hata kama hana tabia bora? Je, kwa nini si vyema kufunga ndoa na watu wasiomwamini Mungu?

**SIKU YA 65**
**(Machi 6)**

# Kitendawili cha Samsoni

**- Waamuzi 14-16**



Samsoni alitoa kitendawili kwa ndugu za mkewe. Kabla hajasema, aliwaambia kuna zawadi ya mavazi 30 ya kitani na mengine 30, jumla yake 60. Wakatega masikio, naye akasema "katika huyo mwenye kula kikatoka chakula, katika huyo mwenye nguvu ukatoka utamu." Zilipita siku saba na hakuna aliyeweza kufumbua kile kitendawili, na wakamwomba yule mke wake ambembeleze Samsoni la sivyo watamteketeza moto yeye na nyumba ya baba yake. Wakasema, "mmetuita ili mpate kuichukua mali yetu? Je! Sivyo?" Basi mkewe Samsoni akamlilia na kusema anamchukia, na wala hampendi kwa vile amewategea kitendawili watu wake Wafilisti naye hakumwambia. Samsoni alisema hajawaambia hata wazazi wake jibu la fumbo, na mke wake akazidi kulia mbele yake kwa siku saba karamu ilipokuwa inaendelea. Siku ya saba mke alisisitiza sana, naye akamwambia jibu la kile kitendawili. Basi huyu mwanamke aliwaambia watu wake lile jibu, siku ya saba kabla ya jua kuchwa. Jawabu la kitendawili lilikuwa, "ni kitu gani kilicho kitamu kuliko asali? Ni kitu gani kilicho na nguvu kuliko simba?" Asali hii ilikuwa katika mzoga wa simba, na simba ana nguvu. Samsoni akasema, "hamkulima na mtamba wangu," yaani, mke wangu amewaambia jibu, la sivyo msingejua.

Roho ya BWANA ikamjia tena Samsoni, naye akaenda Ashkeloni, akapiga wanaume 30, na kuzitwaa nyara zao na kuwapa waliokitambua kitendawili mavazi yao. Akapata hasira tena, naye akaenda kwa wazazi wake, akimwacha mke wake. Basi yule mke wake aliozwa kwa rafiki yake Samsoni. Na baadaye wakati wa mavuno ya ngano, alitokea tena kumtazama mkewe na akichukua mwana mbuzi. Baba mkwe akamzuia kuingia na kusema kwamba, "hakika mimi nilidhani ya kuwa umemchukia kabisa, basi nalimpa rafiki yako. Akasema yule mke wako ana ndugu yake mdogo mzuri zaidi, tafadhali mtwae huyo badala yake. Samsoni akasema, "safari hii 'sitakuwa na hatia katika habari ya hawa Wafilisti, hapo nitakapowaadhibu." Akakamata mbweha 300, na kuwawekea mienge miwili ya moto kwa kila mmoja, na kuwafunga akawaachia mashambani, nao wakateketeza matita ya ngano za Wafilisti kwa sababu ya hasira ya kuchukuliwa mke wake. Wafilisti walienda wakamteketeza mkewe na baba mkwe wake. Basi Samsoni

akasema atajilipiza kisasi na hilo, akawapiga upeo kwa mapigo makuu na kwenda hadi ufa wa jabali la Elamu huko Yuda. Wafilisti walimfuata Samsoni huko na watu wa Yuda walipouliza wanafuata nini wakasema wanamtafuta Samsoni ili kulipiza kisasi. Watu wa Yuda wakamwambia Samsoni kwa nini amefanya hivi na anajua wao ni watumwa wa Wafilisti. Naye akasema analipiza kisasi kwao, wakasema wameshuka kumfunga na kuwapa Wafilisti. Akawaambia wasimwue wao Wayahudi ila mbele ya Wafilisti yeye atajua jinsi ya kufanya. Basi walimfunga kamba mbili mpya na alipofika kwa Wafilisti, Roho ya BWANA ikamjia kwa nguvu na zile kamba mikononi zikakatika juu ya mikono kama vile kitani inavyoteketea na moto. Vifungo vilipoanguka alichukua mfupa wa taya la punda na akapiga watu elfu na kusema tena kitendawili, "kwa taya la punda chungu juu ya chungu. Kwa taya la punda nimepiga watu elfu." Kweli Samsoni alikuwa mtoto wa nadhiri na miujiza, maana mtu mmoja kupiga watu elfu! Alipotupa ule mfupa wa taya Ramath-lehi alisikia kiu kikali, akasikia kufa na akamwita Bwana amsaide "wewe umetupa wokovu huu kwa mkono wa mtumishi Wako; sasa nitakufa kwa kiu." Basi Mungu akapasua shimo mahali, maji yakatoka naye akanywa na kurudisha roho yake na hata akaburudika.

Basi Samsoni hakupata uzoefu wa kutii Sheria za Mungu. Kwa vile tu ndiyo alikuwa amepiga Wafilisti 1000, walipogundua pale alipokuwa walimfuata na wakazunguka nyumba yake wakimvizia usiku kucha wakitaka wamwue. Usiku wa manane Samsoni alitoka na akangoa geti la mji kutoka kwenye bawaba zake na komeo lake akajitwika mabegani mpaka mlima unaokabili Hebroni.

Baada ya hapo aliendа bonde la Soreki na kumpenda mwanamke mmoja aitwaye Delila. Wakuu wa Wafilisti walimwendea Delila ili ambembeleze Samsoni atoe siri ya nguvu zake nyingi na jinsi watakavyoweza kumshinda ili wapate kumfunga na kumtesa. Walimwahidi kumpatia fedha elfu na mia moja. Delila akamtafadhalisha Samsoni amwambie nguvu zake, na jinsi awezavyo kufungwa ateswe. Mara ya kwanza Samsoni alisema, "wakinifunga na kamba saba mbichi zisizokauka nitakuwa dhaifu kama wanadamu wenzangu." Wafilisti wakamletea Delila kamba amfunge mume wake. Alipofanya hivi, mke akamwambia, "Samsoni Wafilisti wanakujia, akazikata zile kamba kama moto ugusavyo pamba. Delila akasema, umenidhihaki na kuniambia uongo tafadhali niambie Ukweli, kwamba unafungwa na kitu gani. Safari ya pili Samsoni akamwambia Delila kwamba yeye akifungwa na kamba mpya ndipo atakuwa dhaifu. Delila alimfunga na kamba mpya na kusema tena, "Samsoni Wafilisti wanakujia." Samsoni hakujua kwamba alikuwa anacheza na Shetani, alikuwa amezama dhambini na kuwa sugu. Basi hata safari hii alizikata kamba hizi kama zimeguswa na moto, na asili ya nguvu zake haikujulikana. Delila akamwambia amemdanya mara ya pili, na akamtafadhalisha "niambie waweza kufungwa na kitu gani?" Mara ya tatu Samsoni alikuwa anasogea kwenye nguvu zake kichwani, akamwambia, "ukivifunga vishungi saba vya nywele za kichwa changu katika mtande wa nguo," Delila akazifunga kwa msumari na kumwambia, "Samsoni Wafilisti wanakujia". Samsoni akaamka usingizini na akaungoa ule msumari na ule mtande. Mwanamke akasema "wawezaje kusema, nakupenda; na moyo wako haupo pamoja nami, umenidhihaki mara hizi tatu, wala hukuniambia asili ya nguvu zako nyingi". Alimsumbua na kumsonga kwa maneno ya kuudhi kila siku, mpaka akataka kufa. Jambo la ajabu ni kwamba hakutoka arudi kwao kwa

Waisraeli na hakuwa gerezani! Yeye alimpenda mwanamke, bali mwanamke hakumpenda kabisa kwani alitaka amwue. Hata leo wengi wamejiweka mtegoni kwa sababu ya wanawake au wanaume wasiompenda Mungu na wamejichoma kwa maumivu mengi na hata kufa kiroho na kimwili.

Sio kwamba Mungu alikubaliana na tabia potofu za Samsoni lakini kama Mshauri wa kweli Hakumwacha Samsoni hata alipoharibu mambo waziwazi. Huwa nashangaa tu jinsi Mungu alivyo na neema. Na kinachoshangaza zaidi kwangu ni jinsi alivyo na neema kwangu. Je, hutaungana nami katika kupiga kelele 'Haleluya!' Lakini kama bado hujafunga ndoa na umejiingiza katika mahusiano usiofaa, kimbia mara moja hapo! Ikiwa umeshafunga ndoa, anza kusali kuliko wakati mwingine wowote, lakini usiiache imani. Mwambie Roho Mtakatifu akuongoze na kumimina upendo wa Mungu ili kumbariki mwenzi wako. Miujiza bado hutokea. Asante, Yesu, kwa kutukomboa kutoka kwa mahusiano mabaya na kuelekeza hatua zetu kwenye njia sahihi! Kuna msemo kwamba upendo ni upofu. Hili si kweli, mahaba ya mihemko au ya ndoto za mchana ndiyo yana upofu (infatuation), upendo wa kweli unatambua na unaenda na kanuni za Mungu na wala si hisia na mihemko tu. Upendo wa kweli una kiasi, usahili, unyofu, maadili, dini na kujitawala nafsi. Mungu aliuruka uchaguzi mbaya wa Samsoni ili kulitimiza kusudi Lake. Hiyo haimaanisha kuwa Aliidhinisha chaguo lake,la! Kwa kuwa Mungu havunji amri Zake Mwenyewe

*Ina maana gani kuomba Katika Jina la Yesu—Kuomba katika Jina la Kristo kunamaanisha mengi. Inamaanisha kwamba tunapaswa kukubali tabia yake, kudhihirisha roho yake, na kufanya kazi zake. Ahadi ya Mwokozi inatolewa kwa masharti. "Mkinipenda," Anasema, "mtazishika amri Zangu." Yeye huwaokoa wanadamu, si katika dhambi, bali kutoka katika dhambi; na wale wanaompenda wataonyesha upendo wao kwa utii.


---

Kwa nini Samsoni alipiga watu 30. Kwa nini Samsoni alibeba geti la mji? Je, rafiki yako wa karibu akikuambia anataka kukuua na kukwambia njia ya kukufunga ungekubali? Je, unafikiri Mungu alitaka Samsoni aishi na wanawake wasioamini? Andika tabia za mke au mume mwenye tabia nzuri. Elezea kisa cha mtu aliyeuwawa na rafiki, mke au mume wake?

**SIKU YA 66**
**(Machi 7)**

# Mwisho wa Samsoni

**–Waamuzi 16**



Samsoni alisumbuliwa na mwanamke. Hakutaja tena kwamba alikuwa anaipigania Israeli, ila mchezo wa paka na panya kwa kuwindana. Ilifika siku akatoa siri kwa Delila. Siri ambayo hata wengi katika Israeli hawakuijua. Akamwambia Delila, "wembe haukupita juu ya kichwa changu kamwe; maana mimi nimekuwa mnadhiri wa Mungu, tangu tumboni mwa mama yangu; nikinyolewa, ndipo nguvu zangu zitanitoka, nami nitakuwa dhaifu, nitakuwa kama wanadamu wenzangu. Delila akajua wazi kwamba safari hii amemwambia yote yaliyokuwa moyoni na akatuma neno kwa wakuu wa kabila lake, Wafilisti, ambao walikuwa maadui wa Israeli na Mungu wa mbinguni. Akawaambia sasa waje mara ya mwisho tu, kwani alikuwa amemwambia yote yaliyo moyoni mwake. Wakuu wa wafilisti walimpa Delila pesa ya kumuuza rafiki yake, Samsoni. Delila akamlaza Samsoni magotini akiwa amesinzia kumlaghai, akawa kama Hawa mbele ya Shetani, na pengine akajitia kumwonesha upendo, naye akamwita mtu kumnyoa, vile vishungi saba vya kichwa chake na akaanza kumsumbua, na nguvu zake zikamtoka. Delila akasema 'Samsoni wafilisti wanakujia, naye Samsoni akaamka sasa akiwa mnyonge na

kusema “nitakwenda nje kama siku nyingine, na kujinyosha, lakini hakujua kwamba BWANA amemwacha kwa sababu ya kuendelea kuipenda dhambi na kuitenda. Basi Wafilisti walimkamata na kung’oa macho yake. Wakaenda naye mpaka Gaza na kumfunga vifungo vya shaba, naye akawa akisaga ngano kwa ajili ya wafungwa gerezani. Lazima wazazi walisikitika kwa kuona mtoto wao, aliyekuwa mnadhiri wa Mungu, akiwa sasa ni kipofu kwa sababu ya kutotii Neno la Mungu na ushauri wa wazazi.

Mungu Mwenye huruma alimsaidia na kukuza nywele zake tena. Nywele zake zikaanza kukua na nguvu zake zilianza kurejea. Ndipo Wafilisti wakafanya sherehe ya kumtolea sadaka mungu wao Dagoni na kufurahi kwamba “mungu wao amemtia Samsoni adui yao mikononi mwao. Walipoona hivyo wakamhimidi huyo mungu. Wakiwa wanashangilia kwenye sikukuu hii, walimwita Samsoni aje afanye michezo. Wakamtoa gerezani ili acheze mbele yao. Samsoni akamwambia kijana aliyemshika amwache azipapase nguzo apate kuzitegemea. Ukumbi huu ulijaa watu wengi, wanaume na wanawake wapatao 3000 wakamtazama Samsoni akicheza. Samsoni akamkumbuka Mungu, na kumwita, “Ee Bwana, Mungu, unikumbuke, nakuomba, ukanitie nguvu, nakuomba mara hii tu, Ee Mungu, ili nipate kujilipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa ajili ya macho yangu mawili.” Mungu ni Mwenye rehema akamsikiliza Samsoni, naye alishika nguzo hizi akazitegemea, kwa mkono wake wa kuume na wa kushoto, kisha akasema, “na nife pamoja na hawa Wafilisti.” Akainama kwa nguvu zake zote na kuzisukuma zile nguzo mbili na jengo likawaangukia wakuu wa Wafilisti waliokuwa wanasherehekea pamoja na wote 3000 wakafa. Wale watu aliowaua wakati wa kufa kwake walikuwa wengi kuliko waliouawa wakati wa uhai wake. Ndugu na wazazi wake wakaenda kuchukua mwili wake na kumzika kwenye kiwanja cha baba yake. Samsoni aliungama. Kujiua ni kuvunja amri ya sita ni dhambi. Aliponea chupu chupu na alipata nafasi ya kuungama na hata leo yupo katika wale wenye imani wa Waebrania 11 na waamuzi wengine “Gideoni, Baraka, na Samsoni na Yeftha.”

Mungu ni mwenye huruma na upendo, lakini tunapaswa kuwa waangalifu, na kutochezea dhambi. Samsoni alikuwa ni mtu mwenye nguvu lakini aliye dhaifu wa tabia. Angefanya makubwa kwa Mungu, lakini aliwapenda wanawake wa maadui na kutoishi maisha ya usafi ya ndoa. Samsoni alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka 20. Alikuwa kiongozi wa nchi, pande na jitu lenye nguvu, lakini aliangushwa na wanawake dhaifu. Wakati tunaona mtoto Yusufu, aliyekuwa mtumwa na mnyonge, akishinda majaribu ya mama Potifa aliyemshika kwa nguvu. Si waoga wakimbiao dhambi, bali mashujaa.
Kimwili, Samsoni alikuwa mtu mwenye nguvu kupita wote duniani; lakini katika kutawala nafsi, uadilifu, na uthabiti, alikuwa mtu dhaifu sana. Ila sala yake ya mwisho bado ilisikika, na jina lake lipo katika Waebrania 11. Je, BWANA anaweza kuokoa waraibu wa ngono, wezi, au watu waovu wanaokufa? Jibu ni rahisi na la kushangaza: Kila mtu atakayeliitia Jina la BWANA ataokolewa Warumi 10:13. Ninamsifu BWANA kwa upendo Wake usio na kikomo na neema Yake ya ajabu leo. Na wewe je? Inanikumbusha maneno ya wimbo “Upendo usio na mwisho wa Mungu usio na kipimo, unanikimbiza ili unipate, unapigana vita kwaajili yangu hadi nimjue na kumpenda.......”. Ninampenda na kuuthamini upendo Wake. “Ee Mungu,

uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu. Usinitenge na uso wako, Wala Roho Wako mtakatifu usiniondolee. Unirudishie furaha ya wokovu Wako; Unitegemeze kwa roho ya wepesi" ( Zaburi 51:10-12 ). Kwa hiyo, haijalishi mitihani au majaribu ni makubwa kiasi gani, sisi tuwe waaminifu kwa Mungu maana ni hapo tu ndipo Yeye awezapo kutimiza ahadi Yake isemayo, "wewe u Wangu. Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendapo katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza." (Isa. 43:1, 2). Acha na tuwe waaminifu Kwake hadi kifo (Ufu. 2:10)!

*Yesu alisema, "Ninyi mtaomba kwa Jina Langu; nami siwaambii, kwamba nitaomba kwa Baba kwa ajili yenu: kwa maana Baba Mwenyewe anawapenda." Nimewachagua: ... ili chochote mtakachomwomba Baba kwa Jina Langu, awapatie. " Yohana 16:26, 27; Yohana 15:16. Lakini kuomba katika Jina la Yesu ni jambo zaidi ya kutaja tu Jina hilo mwanzoni na mwisho wa ombi. Ni kuomba katika akili na roho ya Yesu, huku tukiamini ahadi Zake, kutegemea neema Yake, na kufanya kazi Zake.

---

Kwa nini Samsoni alikubali kuishi na Delila japo hakulazimishwa? Kwa nini Delila alitaka Samsoni atoe siri yake? Nguvu za Samsoni zinakupa fundisho gani ukipewa hizo nguvu? Samsoni alilipizaje kisasi kwa Wafilisti mara ya mwisho? Samsoni aliamua miaka mingapi?

**SIKU YA 67**
**(Machi 8)**

# Hekalu la Sanamu la Mika, uovu wa mtu moja waenea kwenye familia nzima!

**- Waamuzi 17 na 18**

Siku za waamuzi katika Israeli, kulikuwa na mtu aitwaye Mika, aliyeishi katika milima ya Efraimu. Mtu huyo alimchukulia mama yake fedha elfu na mia moja. Mama alipotafuta na kuulizia, Mika alisema kuwa zile pesa za wakfu "tazama, ninazo mimi hizo fedha, ni mimi niliyezitwaa." Mama akamshukuru kijana wake kwa kukiri kosa lake, na Mika akamrudishia mama yake zile pesa, na mama akaamua aziweke wakfu kwa BWANA, ila njia aliyotumia ilikuwa ya uovu. Badala ya kupeleka Shilo kwenye hekalu la BWANA alitumia kununulia sanamu. Akasema, "zitoke mikononi mwangu kwa ajili ya mwanangu, ili kufanya sanamu ya kuchonga, na sanamu ya kusubu, basi kwa hiyo nakurudishia wewe." Yule kijana alipomrudishia mama yake pesa, alitwaa 200 na kumpata fundi ili kufanya sanamu ya kuchonga na ya kusubu, ambazo zilikuwa ndani ya nyumba ya Mika. Mika alikuwa na nyumba ya miungu, naye akajitengenezea nguo za ukuhani na kinyago, akamweka wakfu mmoja miongoni mwa wanawe akawa kuhani wake. Siku hizo hapakuwa na mfalme katika Israeli; kila mtu alifanya hayo aliyoyaona kuwa mema machoni pake mwenyewe.

Akatokea mtu kutoka Bethlehemu ya Yuda, aliyekuwa ni mlawi naye akaa huko hali ya ugeni, na mtu huyo akaenda afikie ugenini katika vilima vya Efraimu. Alifanya safari akafika mpaka kwenye nyumba ya Mika. Mika akamwuliza anatoka wapi na kwenda wapi, akamwambia alipotoka na kwamba anaenda ugeni popote atakapopaona. Mika akamwambia akae pamoja naye, awe baba na kuhani na yeye atamlipa mshahara kwa mwaka kwa nguo ya kuvaa, chakula na fedha kumi kwa mwaka. Yule mlawi akakaa, na kuwa kama mmojawapo wa wanawe. Mika akamweka 'wakfu' naye akawa kuhani. Mika akaridhika na kusema "sasa najua kwamba BWANA atanitendea mema, kwa kuwa nina mlawi kuwa kuhani wangu". Siku hizo zisizo na wafalme Wadani walijitafutia urithi wapate pa kuishi, wakatuma watu mashujaa na kuipeleleza nchi na kuikagua, wakaondoka wakafika vilima vya Efraimu, hata nyumba ya Mika wakalala pale. Pale walimwona yule kuhani bandia na kumwuliza anafanya nini hapa, na "nani amekuleta wewe huku?" Akawaeleza ilivyotokea na wakamwambia awasaidie kupata ushauri toka kwa Mungu kwamba njia wanayoiendea kutafuta ardhi ya kukaa itafanikiwa. Yule kuhani bandia akajibu "haya endeni kwa amani; njia mnayoiendea iko mbele za Bwana." Hawa watu wakaenda Laishi na wakawaona watu walio pale wakiishi maisha ya usalama na kama vile wamejisahau kwani walikaa kwenye starehe na hifadhi. Katika nchi hii hakuna aliyekuwa na amri, aliyeweza kuwatweza katika neno lolote, nao walikuwa kama Wasidoni, yaani, hawakuwa na shughuli na mtu ye yote. Wapelelezi hawa walirudi kwao na kusimulia yale waliyoyakuta huko Laishi. Na wale wenzao Wadani wakashauri waende wakapigane nao "kwa kuwa tumeiona hiyo nchi nayo

ni nchi nzuri sana, nanyi je, mwanyamaa tu? Msiwe wavivu kwenda na kuingia mpate kumiliki nchi hii. Wapelelezi wakaendelea kusema, "mtawafikia watu wakaao salama salimini na hiyo nchi nayo ni kubwa; kwa kuwa Mungu ameitia mikononi mwenu, ni mahali ambapo hapana kupungukiwa na kitu chochote duniani!

Wakatoka watu mia sita wa Dani na kwenda kupiga kambi huko. Wakafika vilima vya Efraimu wakapita huko. Wakamwuliza yule kuhani anaendeleaje, wakaingia ndani na kutwaa hiyo sanamu ya kuchonga na nguo za kuhani (naivera) na kile kinyago na hiyo sanamu ya kusubu, yule kuhani akawauliza wanafanya nini? Ndipo wakasema, "nyamaza wewe, weka mkono wako kinywani mwako, uende pamoja nasi, uwe kwetu baba, tena kuhani." Wakamwambia ni jambo la maana kwake kuwa kuhani wa kabila kubwa kuliko nyumba moja tu.

Moyo wa 'kuhani bandia' huyu ukafurahi. Naye akatwaa hiyo naivera ya kushona na akaenda nao. Wakatanguliza watoto na wanyama wao, na Mika alipowafuata na kulalamika walimwambia "Hiyo sauti yako isisikiwe tena kati yetu, wasije walio na hasira wakakuangukia, nawe ukapotewa na uhai wako" na wa familia yako. Mika akaona wana nguvu kumshinda akarudi zake kwake. Wakaenda mpaka Laishi mji wa starehe na hifadhi, nao hawakuwa na shughuli na mtu awaye yote, na mji huo ulikuwa katika bonde. Pale wakawapiga watu na kuchoma moto mji. Kisha wakajenga mji na kuuita Dani. Na hawa wana wa Dani wakajisimamishia sanamu ya kuchonga na inavyoonekana, mjukuu wa Musa, yaani mwana wa Gershomu ndiye aliyekuwa kuhani wao bandia waliyemnyang'anya Mika. Kweli haikuchukua muda mrefu, wana wa Israeli wakaanza kutomjali Bwana. Hii inatuonesha kwamba daima tumtegemee Mungu ili tusiingie kwenye mitego ya Shetani.

Katika siku zetu za leo tunaona lile fungu la 7:13 likituathiri maisha yetu "Sasa najua kwamba Mwenyezi-Mungu atanifanikisha kwani nina kijana huyu Mlawi kama kuhani wangu." Yaonekana watu hutaka Mungu awabariki huku wakishikilia Miungu au sanamu zao au huku wakijifanyia yaliyo mema machoni mwao, ila si machoni pa Mungu. Hivyo ndivyo Balaamu aliajiriwa kuwalaani Israeli, alitaka kununua baraka kwa masharti yake mwenyewe, Hatuwezi kupuuza amri za Mungu na kudhani tutabarikiwa. Mara nyingi tutafutapo kazi tunaona kama inalipa vizuri, na si kwamba kipato chake ni cha halali. Mbali na sanamu zilizochongwa zinazooonekana, kuna zile mpya zisizokemewa sana, kama vile mitindo, ulevi, fikra potofu, uasherati, kupenda mali, tamaa isiyozuilika, injili ya ustawi, ukosefu wa maadili na mengineyo. Wagalatia 5 inaunganisha kazi za mwili na tunda la Roho ili tuweze kuona tofauti: "Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya: uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu. Kichocheo cha hakika cha machafuko ni wakati kila mtu katika jamii fulani anafanya kile ambacho ni sawa machoni pake mwenyewe, na ndivyo ulimwengu wetu ulivyo sasa. Mungu wetu ni Mungu wa utaratibu Mabishano kati ya Mungu na Shetani yalianza wakati Shetani aliposema hakuna haja ya sheria. Tangu wazazi wetu wa kwanza, Adamu na Hawa, walipomkubali Shetani kama kiongozi wao mambo yamekuwa ya huzuni.

Hakika sheria isipokuwepo, mateso, misiba, maumivu, na kifo huwa ndiyo fungu letu. Ulimwengu wetu ni kitabu cha kiada kwa malimwengu ambayo bado hayajaanguka. Wameona kwamba bila sheria, hakuwezi kuwa na amani, na hakuna uzima. Hivi karibuni, ulimwengu huu wa uasi-sheria utafikia mwisho, na mahali pake patakuwa na nchi ambayo kila mtu atatii sheria ya Mungu kikamilifu—ndiyo maana itaitwa paradiso! Wale ambao watakuwa huko kutoka katika ulimwengu huu wanaitwa " Masalio ya uzao Wake, wale wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo." Ufunuo 12:17

*MUNGU Anatualika Kuja Kwake katika Jina la Yesu—Unaalikwa kuja, kuomba, kutafuta, kubisha; na umehakikishiwa kwamba hautatoka mtupu. Yesu anasema, "Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye hupata; na yeye abishaye atafunguliwa. " Mathayo 7:7, 8 .

---

Je, Mika aliiba pesa toka kwa nani? Alifanyia nini hizo pesa? Yule kuhani alikuwa nani na alikuwa wa ukoo gani? Ni nani aliiba vinyago kwenye hekalu la Mika? Je, watu wale wa Laishi walikuwa na tabia gani? Tabia ya starehe ina athari gani?

**SIKU YA 68**
**(Machi 9)**

# Uovu Unaowasha Masikio Katika Israeli

**- Waamuzi 19-21 (Kipindi cha 1400-1000 KK)**



Siku hizo ambazo hakukuwa na mfalme katika Israeli aliondokea mlawi aliyekaa ugenini katika vilima vya Efraimu na kutwaa mke katika Yuda. Bali yule mwanamke akaanza kwenda kwa wanaume wengine, na huyo mume akamwacha arudi kwao kwa baba mkwe wake. Alikaa kule kwa miezi minne, na mumewe akaenda kumfuata, aseme naye kwa upendo na kumrudisha. Alienda kwa punda na mtumishi, na mwanamke huyu na baba mkwe wake walimkaribisha na wakafurahi kuonana naye. Baba mkwe akamzuia asiende bali akae naye siku tatu. Walikaa wakila na kunywa siku hizo, na asubuhi ya siku ya nne mlawi aliamka aende zake, na kumwambia baba mkwe wake, bali baba mkwe alisema, "tunza moyo wako, ule chakula kidogo, kisha baadaye mtakwenda zenu." Ilipofika mchana, baba mkwe akakazana tena kwamba akae mpaka usiku kucha na moyo wake ufurahi. Siku ya tano aliamka tena na kutaka kwenda na mke wake, lakini baba mkwe akasema vilevile, kwamba aende jua likipinduka. Ilipofika jioni, akitaka kuondoka, baba mkwe akasema mchana umeisha na jioni imekaribia, lala hapa, uende kesho asubuhi na mapema. Kweli watu wa siku hizo walijua kuwakarimu wageni, siku hizi wengine wanaogopa wageni, hata wakimwambia mtu aje, akikataa wanafurahi kwamba mzigo umepungua. Au katika jamii zingine, wengine husema nakukaribisha kwangu, ila uje na chakula chako.

Siku hii huyu mlawi alinuia na kusema, "wala sitalala hapa leo, japo ni jioni." Akaenda na kufika Gibea, kwa punda na mke wake na mtenda kazi mmoja. Ikawa jioni na wanahitaji kulala wakakaa mjini kwenye njia ili mtu yeyote awakaribishe. Ndipo akatokea mtu mume mzee akitokea shambani na kuwaambia, kwamba anatoka vilima vya Efraimu, na anakaa Gibea kama mgeni. Ila wenyeji wa mji pale walikuwa Wabenyamini. Alipoangalia aliona wasafiri hawa katika njia kuu ya mjini akawauliza, wanatoka wapi na wanakwenda wapi? Wakamweleza. Mtu huyu Mlawi alisema ana chakula cha mifugo yake, na chao na, ni mahali tu pa kulala panakosa. Mzee huyu akasema, wawe na amani moyoni, yanayowapungukia atawasaidia, ila wasilale njiani. Akawaleta nyumbani mwake na akawapa punda wao chakula, akawaosha miguu nao wakala na kunywa. Wakati wakifurahisha

mioyo yao wakaja watu mabaradhuli, waovu wa mji, wakaomba wamlete yule mtu, kwani walikuwa ni mashoga, yaani watu wenye kutaka urafiki mbaya na wanaume wenzao. Jambo hili ni machukizo mbele za Bwana, ni dhambi kama dhambi zingine. Mtu yule akazungumza kama Lutu, kwamba yeye ndiye mwenyeji, hawezi kuwaachia hawa wageni wapate madhara hivyo, bora wapate watoto wake. Watu hawa hawakusikia, na yule mtu wa Lawi akamtoa mke wake na kumleta kwao watu hawa, nao watu hawa wakamtendea uovu usiku ule. Hii inaonyesha kuwa utamaduni huo haukumthamini mwanamke anavyopaswa kuthaminiwa. Alifia kwenye mlango wa mwenyeji wao, na ndipo yule Mlawi kwa masikitiko alimchukua mke wake na kumweka juu ya punda na kwenda mahali pake, kisha akauchukua mwili wa yule mke wake na kuukata vipande 12 na kutuma kila kipande kwenye kabila la Israeli. Watu walipoona mambo haya wakajua uovu wa Israeli umepita mipaka, kwani watu wamekuwa kama wanyama sasa, wakanena "jambo kama hili halijatendeka wala kuonekana tangu siku hiyo wana wa Israeli walipokwea kutoka katika nchi ya Misri hata leo; haya lifikirini, fanyeni shauri, mkanene".

Makabila ya Israeli yalifanya mkutano wa watu na kuamua wawapige Benyamini ndugu zao, kwani wanastahili adhabu kwa uovu huu ambao ungeifanya Israeli ipate laana. Walimwuliza Mlawi kilichotokea naye akaelezea na kusema, "nyote sasa Israeli toeni mashauri yenu." Watu wakasema watakwea Gibea na kuwapiga. Ila kwanza walituma ujumbe Gibea wawatoe hao mabaradhuli ili wapate kuuawa na kuondoa aibu katika Israeli. Wabenyamini walipokusanyika, walitaka kupigana na si suluhu, au kuondoa hawa waovu ili wengi wasife.

Benyamini walikuwa na askari 26,000 na walikuwa tayari kupigana na jeshi la Israeli la watu 400,000. Kabla ya kwenda vitani, Waisraeli walimwomba Mungu ili kujua ni kabila gani kati ya makabila hayo walipaswa kushambulia kabila la Benyamini kwanza. Mungu alisema "Yuda watakwea kwanza." Lakini katika vita vya kwanza, Benyamini waliwashinda Waisraeli na kuwaua Waisraeli 22,000. Katika vita vya pili, Israeli ilishindwa tena, na kupoteza askari 18,000. Waisraeli wakalia na kulia hata jioni mbele za BWANA kwa vile vilikuwa ni vita vya kupigana na ndugu zao. Vita hii iliendelea mpaka Waisraeli wakaamua waunguze mji wa Benyamini, na kuwazingira na kuwafukuza. Jambo la kusikitisha, kwamba watu hawapo tayari kuungama ili wasiangamie, bali wanataka kupigana. Basi wanaume karibu wote wa Benyamini wakaisha, na Israeli ilipokaa pamoja tena waliamua wasiwape Benyamini mabinti zao. Wakalia, "Ee BWANA Mungu wa Israeli, kwani jambo hili kuwa katika Israeli, ya kwamba hivi leo kabila moja limepunguka katika Israeli?"Walitoa dhabihu na sakaka kwa BWANA na kumkaribia BWANA. Walijaribu kuwatafutia wanaume 400 waliobaki wake kutoka Yabesh-Gileadi ili Benyamini isipukutike kabisa, katika makabila ya Israeli. Wanaume wengine waliokosa wanawake walitafuta kwa njia ya ajabu kabisa, yaani wakiona wasichana wanatoka kwenye sikukuu, wakicheza michezo wakati wa mavuno, wawanyakue. Na baba au ndugu za wasichana wakija watoe samahani na kuwaeleza shida iliyotokea. Benyamini ilinusurika! Maana hata mtume Paulo baadaye alitoka kabila la Benyamini. Uovu anaofanya binadamu unaleta madhara makubwa. Tumuombe Mungu atupatie ushindi dhidi ya uovu na dhambi.

Wakati watu walipofanya yaliyo mema machoni pao, wabenyamini wakakosa wanawake wa kuoa kama kisa kinavyoelezea nao Badala ya kuchumbia wanawake kama vile Maandiko yanavyosema, wao wakajifanyia wanavyotaka. Hawakulinda haki na heshima za wasichana, Wakaenda kuwavizia na kuwateka ili wawe wake! Mtazamo wa binadamu hakika unajiletea huzuni, kwani hakuna msichana anayetaka kuporwa akiwa anachota maji ili akawe mke wa mtu. Hali kama hii isipodhibitiwa itapelekea wanawake na watoto kunyanyaswa. Wasichana na watoto wadogo wasio na ufahamu na walio katika mazingira magumu watatumikishwa na kubakwa kama tulivyoona awali kwenye kisa hiki. Kutokuwa waaminifu katika taratibu za Mungu, hufanya maadili yote kutupwa nje kwa urahisi, na orodha ya maovu itaendelea kuzidi. Lakini tunaweza kuepuka haya yote ikiwa tutamfanya Mungu awe Mfalme wa maisha yetu, Hebu tujichunguze mioyo yetu na kujiuliza, Je, ninamtii Mungu kwasababu nampenda au kwasababu ni lazima nimtii?

Tunamshukuru Mungu kwa uvumilivu Wake, subira na huruma Yake. Ikiwa Asingekuwa na sifa hizi, Angewaangamiza wanadamu wote, wala hakuna mtu angebakia. Lakini upendo Wake hauna masharti, yaani Agape, ni wa milele, na wa kujitoa. Na ndio maana bado anatuhurumia, anatutunza na anatujali, akitumaini kwamba ndani ya kipindi cha rehema alichompa kila mmoja wetu (miaka sabini hadi themanini), na ulimwengu wetu, tutatubu na kukubali zawadi Yake ya uzima wa milele. Tulipata rehema hii kupitia Kristo Yesu. Mwanadamu yeyote akipotea, swali ambalo Mungu atamwuliza siku ya hukumu ni, “Kwa nini ulikataa upendo?”

Kisa cha Waamuzi ni taswira ya mapambano kati ya imani na mapokeo. Nayo imani ikapotea na desturi ikabakia. Kisa hiki cha kutisha ni picha ya taifa la Mungu, ambalo watu walifanya yaliyo sawa machoni pao wenyewe. Wakati watu wanaishi kwa ajili ya kile tu wanachohisi kuwa ndiyo sawa, bila kuhamasishwa tena na dira ya maadili ya Mwenyezi Mungu, upotovu wa kuogofya ni matokeo. Cha kusikitisha ni kwamba, upumbavu na uasherati wa kutisha ni jambo la kawaida katika mizunguko ya habari ya leo. Mtu hawezi kusoma Waamuzi 19 bila kustuka au kutetemeka. Hata hivyo visa vinavyofanana vinarudiwa kwa njia mbalimbali kila siku duniani kote, na hata kanisani. Visa hivi vinasimuliwa kwa vyombo vya habari na hivyo vinatufikia kwa wingi zaidi. Ni wanaume wangapi, wanaotaka kujilinda au kulinda haki zao, na kisha huwaweka wanawake katika aina mbalimbali za unyanyasaji? Wanawake waliofanyiwa ukatili, na wanaume pia, bado wananyoosha mikono yao, wakiomba rehema. Je, sisi tutawasikiliza? Mwishowe tunaona kuwa Wanaisraeli katika unafiki wao, hawakutambua kwamba walikuwa na bidii zaidi katika kuwaangamiza ndugu zao kwa ajili ya dhambi zao kuliko walivyokuwa katika utakaso na kuondoa dhambi zao wenyewe. Je, hilo halipaswi kuwa somo kwetu? Hakika ni Mungu na Njia Yake ndiyo ufumbuzi wa shida za mwanadamu, bila Yeye, hatuna matumaini.

*Kristo anaonyesha nia ya MUNGU kubariki kwa utayari wa baba kutimiza ombi la mtoto Wake. Anasema,”Je, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye mtoto wake akimwomba mkate, atampa jiwe?” au akimwomba samaki atampa nyoka badala ya samaki? Na kama akimwomba yai, je, atampa ng’e? Ikiwa basi ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, si zaidi sana Baba yenu wa mbinguni atawapa Roho Mtakatifu hao wamwombao? Luka 11:11-13.

Baba mkwe alimwambiaje yule mtu aliyerudi kuchukua mke wake? Je, Mungu aliruhusu kabila gani liadhibiwe na ndugu zao Israeli? Kwa nini uovu huu ulitokea kila mara Israeli kuliko wakati wa Musa na Yoshua? Kushindwa kwetu mara zingine ni mbaraka, kwa vipi?

**SIKU YA 69**
**(Machi 9)**

# Naomi Arejea Nyumbani Mkamwana Aliyempenda aenda naye

**- Ruthu 1**



Zamani, enzi zile za Waamuzi ambapo kuna historia tele ya kupungukiwa na utukufu wa Mungu na mambo ya kuogofya, kipo kisa cha kutia matumaini kwa binti aliyekuwa wa kabila la adui, kwa Israeli. Palikuwa na njaa katika nchi na mtu mmoja aitwaye Elimeleki wa Bethlehemu ya Yuda aliondoka na mke wake Naomi na watoto wake wawili wa kiume, Maloni na Kilioni kwenda kuishi Moabu. Watoto wake wa kiume wakaoa wanawake wa Kimoabu, mmoja aliitwa Orpa na mwingine Ruthu. Walikaa huko miaka kumi na Elimeleki, Maloni na Kilioni wakafa. Ndipo Naomi alipoondoka na wakamwana wake ili kurudi katika nchi yake, katika mji wa Bethlehemu maana alisikia Mungu amewajilia watu Wake na njaa imekoma. Wakashika njia kurudi, lakini Naomi aliona itakuwa ubinafsi kuwaambia wasichana hawa kuiacha nchi yao kabisa, kwani wangeweza kuolewa tena kwao maana hawakuwa wazee. Akawaambia Orpa na Ruthu warejee kila mmoja nyumbani kwao na akasema, “BWANA awatendee mema ninyi, kama ninyi mlivyowatendea mema hao waliofariki na mimi pia. BWANA na awajalie kuona raha kila mmoja nyumbani kwa mumewe.” Wakweze walipaza sauti na kulia, kweli huyu mama mkwe alikuwa na upendo na walipendana naye. Jambo hili ni la kujifunza hata leo, jinsi ya kuishi na mama mkwe, wakamwana, mawifi, mashemeji, ndugu au hata washiriki. Naomi ni mfano bora, kwani wakweze walisema, “La! sivyo; lakini tutarudi pamoja nawe

kwa watu wako." Naomi akawasihi warejee, alisisitiza "kwa nini kufuatana nami?" Akawaeleza kuwa hakuwa tena na watoto wa kiume ambao wangewaoa, na hata angezaa tena, wao ni watu wazima wasingesubiri mpaka hao wavulana wakue, na hata pengine asingezaa wavulana!

Basi Naomi akasema, maisha yake ni magumu kuliko yao, kwani amefiwa na watoto wawili na mume na tena ni mzee. Wajane wote watatu, wakapaza sauti zao na kulia. Kisha Orpa akambusu mama mkwe wake na kuagana naye. Naomi akamtazama Ruthu na kumwambia mwenzako amerudi kwa watu wake, na mungu wake; basi urejee wewe umfuate urudi naye. Hapo ndipo Ruthu aliposema maneno ambayo yamekuwa yakiakisiwa katika maneno ya bwana na bibi arusi wakati wa kufungiwa ndoa. Ruthu akamwambia mama mkwe maneno haya, "Usinisihi nikuache, Nirejee nisifuatane nawe; maana uendako nitakwenda, na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu. Na Mungu wako atakuwa Mungu wangu; Pale utakapokufa nitakufa nami, Na papo hapo nitazikwa; BWANA anitende vivyo na kuzidi, ila kufa tu kutatutega wewe nami." Basi Naomi aliona binti huyu wa Moabu amekazana mno, akaacha kukazania arudi kwao Moabu. Inawezekana Ruthu aliona Mungu wa Israeli ni wa kweli, na anastahili kumfuata ukilinganisha na miungu ya Moabu. Wakasafiri mpaka wakafika Bethlehemu. Wale watu waliomfahamu Naomi wakajiuliza ni Naomi kweli? "Je! Huyu ni Naomi?" Akawaambia wasimwite Naomi, bali Mara maana ametendewa machungu mno. Akawakumbusha jinsi alivyoondoka akiwa amejaa na sasa hakuwa na kitu." Walifika na mkwe wake Ruthu wakati wa mavuno ya Shayiri na hili likawa baraka kupata chakula na hata kufanya kazi ili kuondoa mawazo mengi. Hata hivyo, Mungu alikuwa na zawadi kubwa zaidi kwao kwenye shamba hilo!



Naomi alikuwa na ndugu ya mumewe, mtu mwenye cheo na mali kwenye mji huo aliyeitwa Boazi. Huyu alikuwa mjukuu wa Rahabu, yule aliyewasaidia wapelelezi kuingia Yeriko. Naomi akamwambia Ruthu aende kuokota masazo ya chakula kondeni. Siku hizo ilikuwa ni sheria katika Israeli, kwamba mtu akivuna, aache masazo kwa watu maskini ili wapate kuokota. Ruthu alienda kukusanya masazo mpaka akafikia shamba la Boazi. Boazi alitoka mjini na kuwaamkia wavunaji "BWANA akae nanyi". Wavunaji walipojibu, Boazi akamwuliza mtumishi wake anayesimamia kwamba huyu msichana mgeni ni nani? Akaambiwa ni yule msichana Mmoabi aliyerudi na ndugu yao Naomi, aliomba aruhusiwe akusanye masazo nyuma ya wavunaji kati ya miganda. Watumishi wakamsifu Ruthu kuwa ni msichana mwenye bidii, "ameshinda tangu asubuhi hata sasa, isipokuwa alikaa nyumbani kitambo kidogo." Boazi alikuwa mtu mzima kwa Ruthu na akamwambia "Mwanangu, sikiliza; wewe usiende kuokota masazo katika shamba lingine, wala usiondoke hapa," akamwambia akae karibu na wasichana wake. Alimsaidia kwa usalama pia ili asipate shida au hatari kwa kuwa kwenye mashamba ya watu waovu. Akamwambia aendelee tu pale, na akawaambia wale wanaume pale wamtendee

vyema kwa uungwana, na akitaka maji anywe kwenye mitungi yao. Ruthu akainama na kushukuru. Alisema, "jinsi gani nimepata kibali machoni pako hata ukanifahamu mimi mgeni?" Boazi akamwambia, "nimeelezwa sana yote uliyomfanyia mkweo, tangu alipokufa mumeo; na jinsi ulivyowaacha baba yako na mama yako, na nchi uliyozaliwa, ukawafikilia watu usiowajua." Ruthu alikuwa amejitoa kwa ajili ya mkwewe. Hakujua kitatokea nini ugenini, na kabila lilikuwa adui wa Israeli ila aliamua kumfuata mama mkwe wake na Mungu wa Israeli." Fadhili, uaminifu, na uwezo wa kufarijiana katika misiba ya maisha ni viungo muhimu vya kila mahusiano yenye afya. Je, fadhili zako, uaminifu na faraja zitaimarishaje mahusiano muhimu uliyo nayo leo? Ruti hakukata tamaa. Na tujifunze utunzaji wa Mungu hatak wenye nyakati ngumu, na kufurahia baraka na fadhili hata wakati tunapobeba mzigo mzito. Tunaweza kujaribiwa kuamini kwamba Mungu ametuacha, lakini hajatuacha. Hatujaona mwisho wa kisa cha maisha yetu kama Mungu aonavyo, na hakika kuna ushahidi karibu nasi wa wema Wake kwetu. Mungu anatamani tumtumaini na kumfurahia kama Baba yetu anayetutakia mema.

Fadhila, uaminifu, na kufarijiana tunapopata misiba ya maisha ni viungo muhimu vya kila mahusiano mazuri. Je! Fadhila zako, uaminifu na faraja zitaimarishaje mahusiano yako muhimu leo? Kisa hiki cha Ruthu kilitokea wakati wa waamuzi. Wakati wa vurugu, ukatili na uvunjaji wa sheria. Ni rahisi kuzama kwenye unyonge wetu wakati wa changamoto. Mungu alikuwa tayari kumwonyesha Naomi kwamba anamjali na ataendelea kumtunza katika uzee wake. Hebu tujifunze utunzaji wa Mungu hata chini ya nyakati mbaya, na kufurahia baraka na fadhili hata wakati wa kubeba mzigo mzito. Tunaweza kujaribiwa kuamini kuwa Mungu ametuacha, lakini hajafanya hivyo. Hatujaona mwisho wa kisa cha maisha yetu bado, tuombe tufunguliwe macho na kuona wema Wake kwetu. Mungu anatamani tumwamini na tumfurahie. Wakati wanaisraeli wengi wakifanya ibada ya sanamu, Ruthu alitambulishwa kwa Mungu wa Mbinguni, na aliamua kubaki mwaminifu kwa Mungu, kwa gharama yoyote. Yesu anasema, "Mimi ni Ufufuo na Uzima, yeye anayeniamini, ingawa amekufa, bado ataishi." Lazima tuwe tayari kufa kwa ajili ya Kristo. Hebu tuhakikishe kwamba tutakuwa miongoni mwa wale ambao watakuwa waaminifu kwa Mungu hadi mwisho kabisa. Hii inawezekana ikiwa tunamruhusu Yesu kutushikilia mikono yetu (Isaya 41:10).

*Tunamwendea MUNGU katika Jina la Yesu kwa mwaliko maalum, Naye anatukaribisha kwenye chumba Chake cha faragha cha kusikiliza maombi. Anaikabidhi ile nafsi iliyonyenyekea, iliyotubu, katika ile imani ya Kristo ambayo kwayo anahesabiwa haki. Yesu anafuta uovu wake kama wingu zito, na moyo uliofarijiwa unapaza sauti kwa kushangilia, "Ee Bwana, nitakusifu; ingawa ulinikasirikia, hasira Yako imegeuka, na umenifariji. Isaya 12:1.

---

Mume wa Naomi aliitwa nani? Kwa nini walienda Moabu? Waliishi miaka mingapi Moabu? Mkamwana aliyerudi Moabu aliitwa nani? Kwa nini watu waliruhusu wengine kukusanya masazo ya shamba? Leo watu wanapaswa kufanya nini kusaidia wenye mahitaji kama siku zile? Naomi alisemaje alipoona Ruthu ameleta chakula alichookota? Boazi alipata habari za namna gani kuhusu Ruthu?

**SIKU YA 70**
**(Machi 10)**

# Boazi Amwoa Ruthu

**- Ruthu 2-4**

Boazi alimbariki Ruthu na kusema, BWANA akujazi kwa kazi yako, nawe upewe thawabu kamili na BWANA, Mungu wa Israeli, ambaye umekuja kukimbilia chini ya mbawa zake. Naye Ruthu alijibu, “bwana wangu, na nipate kibali machoni pako; kwa sababu wewe umeniburudisha moyo, na kumwambia mema mjakazi wako, ingawa mimi si kama mmojawapo wa wajakazi wako.” Wakati wa chakula ulipofika Boazi alimkaribisha Ruthu aje kula na watu wake mkate na siki, na akaketi pamoja na wavunaji, na wakampitishia nafaka za kuoka kama bisi. Alikula, akashiba na kusaza. Boazi akawaambia watenda kazi kwamba wamwache aokote hata kati ya miganda wala msimkemee, “tena mtoleeni kidogo katika matita na kukiacha, na akiokote wala msimkataze.” Ruthu aliokota masazo mpaka jioni na akazipura zile nafaka, na akapata nafaka efa moja, ambayo inazidi ndoo kubwa hivi au lita 22 za ujazo. Alijitwika na kwenda kwa mama mkwe wake, na chakula kile ambacho kilibakia, alipomwonesha nafaka nyingi aliyopata alishangaa. Akamwuliza “Je, umeokota wapi leo?” Abarikiwe huyo mtu huyo mkarimu, aliyetusaidia hivi leo. Ruthu akaeleza habari za Boazi. Naomi akamshukuru Mungu mpaji, na kumwambia Ruthu kwamba huyu mtu ni jamaa yao wa karibu kiukoo.

Naomi, alimpenda sana Ruthu na akamwambia, “Je, Mwanangu, si vizuri nikutafutie raha, ili upate mema?” Kwa desturi zao, mtu akifiwa na mume ilikuwa jukumu la ukoo kumtafutia mwanamke huyo mume wa kuolewa naye. Basi Naomi akasema Boazi ni jamaa wa karibu, hivyo usiku wa leo akiwa anapepeta shayiri ugani, wewe oga na ujipake mafuta na ujivike mavazi yako mazuri uende, ila usijionyeshe kwa mtu. Wakati wa kulala, Boazi akilala uangalie mahali pale na uingie na kulala karibu na miguu yake, naye atakwambia utakalolifanya. Hii ilikuwa ni desturi ya siku zile, na haikuwa kwa ubaya au uchafu. Basi Ruthu alikuwa tayari kufanya yale mama mkwe aliyomwambia. Alikwenda ugani na akafanya vile. Boazi alipokula na kunywa, alienda kulala penye mwisho wa chungu ya nafaka. Hii ilifanyika wakati wa kazi za mavuno, watu hawakulala ndani. Ruthu aliendа na kulala kwenye miguu yake na kulala mpaka usiku wa manane Boazi aliposhtuka aliuliza, “Ama! ni nani wewe?” Ruthu alijitambulisha, na Boazi alijua hiyo ina maana gani kwenye mila zao, na akamwambia Ruthu kwa upendo, “mwanangu, ubarikiwe na BWANA,” umezidi kuonyesha wema kwa kutokimbia na vijana maskini na matajiri. “Usiogope, mimi nitakufanyia yote unenayo, kwa maana wote mjini wanakujua ya kwamba u mwanamke mwema.”

Akamwambia ni kweli mimi ni jamaa yako aliye karibu, ila kuna aliye karibu kuliko mimi. Akamwambia angoje kukicha, nitamwuliza kama yuko tayari kufanya impasavyo jamaa wa karibu, lakini ikiwa hataki, basi mimi nitakufanyia ipasavyo. Boazi alikuwa mtu mwenye hekima wa kufuata hatua zinavyotakiwa na kumpongeza

yule anayejitahidi kutenda mema. Boazi alikuwa mtu wa haki asiyependa sifa mbaya, maana alimchukulia Ruthu kama shemeji yake mdogo na akamheshimu. Yaonekana alipendwa na wafanyakazi wake pia. Akamwambia Ruthu alete shela yake na akamwekea shayiri vipimo sita na kwenda zake mjini. Aliporudi, Naomi alimwuliza mambo yalivyokwenda na akamweleza yaliyotokea na zawadi aliyopewa akaambiwa "usiende kwa mkweo mikono mitupu." Naomi akaona kweli Boazi ni mtu mwenye hekima na upendo, akajua Boazi hatatulia mpaka amelitatua hilo tatizo.



Boazi aliendа langoni mwa mji na kumpata jamaa wa karibu wa mume wa Ruthu na akawaita watu kumi kwa ushahidi na kumwambia mtu huyu kama yupo tayari kumrithi Ruthu au kuwa mume wake, maana ndiyo ilikuwa desturi. Ilikuwa mtu atakayemrithi mke, hurithi na ardhi yake. Mtu huyu alikuwa tayari na mke, bali alitaka kukomboa ardhi tu, akasema "nitaikomboa mimi." Lakini alipoambiwa siku ile atakapolinunua shamba mkononi mwa Naomi, ndio pia amtamchukua Ruthu Mmoabu kuwa mke wake ili amwinulie marehemu jina katika urithi wake kwa kuwa hakuwa na mtoto. Mtu huyo alisema, "mimi sitaweza kulikomboa kwa nafsi yangu, nisije nikauharibu urithi wangu mwenyewe; basi haki yangu ya kulikomboa ujichukulie wewe, maana mimi sitaweza kulikomboa." Basi siku zile kuweka sahihi ya makubaliano ya namna ile, ni kwamba yule aliyekataa kumsaidia ndugu yake kwa urithi alivua kiatu na kumpa mwenzake" kama ushahidi.

Hata leo watu wa mashariki ya kati, wakiona kwamba wewe si mtu mwema huvua kiatu na kukutupia. Naye Boazi akasema kama mlivyoona huo ni ushahidi kwamba atanunua vyote vya Elimeleki, Kilioni na Maloni mkononi mwa Naomi, na pia atalipa mahari ya Ruthu Mmoabi awe mke wake kwa makusudi ya kumwinulia marehemu jina, ili lisikatike miongoni mwa ndugu zake. Wazee waliposhuhudia, wakasema, Bwana amfanye Ruthu kuwa kama "Raheli na Lea" walioijenga nyumba ya Israeli. Boazi akamtwaa Ruthu kuwa mke wake Naye BWANA akawapa mtoto wa kiume aliyeitwa Obedi. Wanawake wakamshangilia Naomi wakisema, "ahimidiwe BWANA, asiyekuacha leo hali huna wa jamaa aliye karibu." Wakambariki wakisema, "jina la mtoto huyu na liwe kubwa katika Israeli." Wakaona Ruthu anamfaa mama mkwe wake kupita watoto saba. Naomi, bibi mtu akamtwaa mtoto Obedi na kumlea. Huyu ndiye baba wa Yese na Yese ndiye aliyemzaa Daudi, na Daudi akamzaa Sulemani. Naomi alipata kicheko na Ruthu akawa mama wa wafalme. Ruthu anatajwa katika vitabu vya injili kwenye mbari ya Yesu. Mambo ya Mungu ni ya ajabu, kwani Rahabu, Ruthu, Mariamu, Bathsheba na Tamari, wanawake walio katika ukoo wa Yesu, walipitia mengi ya kushangaza mno! Hata shomoro mmoja haanguki bila Mungu kujua. Mambo yote hufanya kazi pamoja kwa wema kwa wale wanaompenda Mungu, Warumi 8:28. Kwa hiyo, Tunapoomba ili wagonjwa wapone, haijalishi kile kitakachotokea, tusipoteze imani kwa Mungu.

Ikiwa tunaitwa kukutana na msiba, na tupokee kikombe kichungu, tukikumbuka kwamba mkono wa Baba yetu wa mbinguni unakishikilia kikombe hicho midomoni mwetu.

Lakini kwa nini mwanamke mwema kama Ruthu apate msiba wa kuwa mjane hata kabla ya kupata mtoto? Jibu litatolewa tunapokutana na Kristo uso kwa uso! Kikaango cha mateso kinaweza kuwa kikali sana hata tukahisi tumeachwa na Mungu, lakini anatuambia "Sitakuacha kamwe wala sitakuacha." Waebrania 13:5 . Ruthu alipata jaribu kubwa, lakini Mungu alithibitisha kwamba hajamwacha. Hakika Hamwachi hata mmoja wa watoto Wake! Je, Wakati mtu kutoka nchi nyingine anapowasili kanisani kwako au mahali pa kazi, au anakuwa sehemu ya familia yako, unamkaribishaje na kumbariki kwa wema, heshima na ukarimu wako? Matendo yako ya kukaribisha kwa ukarimu yanafunza nini wale walio karibu nawe? Tunapowasaidia maskini, tunamsaidia Yesu Kristo, kwani atasema siku ya hukumu: "Nalikuwa na njaa mkanipa chakula; nilikuwa na kiu mkaninywesha; nalikuwa mgeni mkanikaribisha; nilikuwa uchi nanyi mkanivika; nalikuwa mgonjwa nanyi mkanitembelea; nilikuwa gerezani nanyi mkaja Kwangu." Mathayo 25:35-36.

*Omba katika Jina la Yesu na kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu — Wakati mtu anatoa ombi la dhati kwa MUNGU (Yesu Kristo Ndilo Jina pekee tulilopewa chini ya mbingu litupasalo kuokolewa), katika ile nguvu na unyofu kuna ahadi kutoka kwa MUNGU kwamba Yupo karibu kujibu hilo ombi na zaidi, juu ya yote tunayoweza kumuomba au kufikiri. Hatupaswi kuomba tu katika Jina la Yesu, bali kwa uvuvio na uwepo wa joto la Roho Mtakatifu. Hii inaelezea kuwa kuna maana gani kusema, "Roho Mwenyewe hutuombea kwa maumivu/kuugua kwingi kusikoweza kutamkika." Maombi lazima yatolewe kwa imani ya dhati. Kisha yatakifikia kiti cha rehema. Endelea kuomba bila kusita au kuchoka. MUNGU hasemi, Omba mara moja, Nami nitakujibu. Neno Lake ni omba, kuwa mwepesi kuomba yaani uwe na utayari (mgambo) wa kutoa sala wakati wowote, ukiamini kwamba umeshavipokea vile vitu ambavyo umeviomba, nawe utavipokea; Mimi Nitakujibu.

*Kwa Jina la Yesu tunaweza kwenda mbele za uwepo wa MUNGU na ujasiri wa mtoto. Hakuna mtu anayehitajika kufanya kazi kama mpatanishi. Kupitia Yesu tunaweza kufungua mioyo yetu kwa MUNGU kama kwa Yule anayetujua na kutupenda sisi.


---

Kwa nini mtu alirithi mke wa nduguye aliyekufa wakati ule? Kwa nini Boazi alienda penye lango la mji? Je, Naomi alipata kazi gani kwa Ruthu na Boazi? Kwa nini watu walimshangilia Naomi? Taja majina matano ya wanawake waliotajwa kwenye mbari ya Yesu. Kwanini mama mkwe ni mama? Kuna uhusiano gani kati ya Boazi, Masini na Yusufu mume wa Mariamu? Je, Mungu amegeuzaje majanga unayoyajua yakawa kizuri kisichotarajiwa?

**SIKU YA 71**
**(Machi 11)**

# Mtoto Samweli, Baraka na Ya Mama Anayeomba na Kumcha Mungu

**– 1 Samweli 1-3**



Palikuwa na mtu mmoja huko Rama, katika nchi ya vilima ya Efraimu ambaye jina lake aliitwa Elkana na mkewe Hana. Hana hakuwa na mtoto. Ndipo Elkana akachukua mke wa pili aliyeitwa Penina. Mtu huyu aliendа kuabudu na kutoa sadaka kila mwaka huko Shilo, na wale wana wa kuhani mkuu Eli, Hofni na Finehasi walikuwako huko. Kila walipoenda kuabudu aliwapatia wake zake sadaka, na mara zote alimpa Hana sadaka mara mbili zaidi, kwa maana alimpenda sana Hana, ingawa alikuwa hana mtoto. Mara nyingi Penina, mke mwenzake alimchokoza na kumdhihaki kwa kutozaa kwake. Hili lilimwaibisha na kumsikitisha sana hata kumfanya alie machozi. Kumwaibisha mtu aliye na shida, kilema, ugonjwa, au masumbufu fulani ni dhambi. Mume wao alipoona hali hiyo alijaribu kumbembeleza Hana na kumwambia jinsi alivyompenda na kuuliza analia nini? Mbona huli chakula, kwa nini moyo wako una huzuni? “Je, Mimi si bora kwako kuliko watoto kumi? Wale wasiokuwa na mtoto wana wakati mgumu. Tunasisitiza kuwa watoto si ndoa bali ni zawadi inayotoka kwa Mungu. Mume na mke hawatoi watoto bali wanapewa na Bwana. Ndoa inaendelea kuwa ndoa hata bila watoto, kwani ndoa na watoto ni vitu viwili tofauti, japo watoto huongeza furaha katika ndoa. Hivyo kuacha mke au mume kwa vile hazai ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Hata hivyo ni nani ajuaye kwamba watoto hawa watakuwa mfano bora au watakusononesha kama Hofni na Finehasi!

Wakiwa Shilo, Hana kwa uchungu rohoni mwake, alimwomba BWANA kwa kulia sana. Aliweka nadhiri kwa Mungu kwamba kama akimpatia mtoto, na kuangalia mateso yake yeye mjakazi wake, na kumkumbuka kwa kumpatia mtoto

wa kiume, ndipo, “nami nitakapompa BWANA huyo mtoto siku zote za maisha yake, wala wembe hautamfikilia kichwani kamwe”, yaani, atakuwa mnadhiri wa BWANA. Mnadhiri ni mtu aliyetengwa au kuwekwa wakfu kufanya kazi maalumu kwa BWANA. Unadhiri unaanzia toka tumboni, utotoni, na ukubwani. Yeremia aliambiwa kuwa toka akiwa tumboni mwa mama yake BWANA alimchagua. Kuhani mkuu Eli, alipoona huyu mama anajisemesha mwenyewe hekaluni alifikiri kwamba amelewa na kuanza kumgombeza maana hakusikia sauti yake. Hana alikuwa akinena moyoni mwake uchungu wake ili BWANA tu ajue. Maana hata mume wake hakuelewa. Kuhani Eli akasema, “Utakuwa mlevi mpaka lini?” Hana akamwambia, hakulewa ila ana uchungu moyoni na anamimina roho yake mbele za BWANA. Akamsihi Eli akisema, “usimdhanie mjakazi wako kuwa ni mwanamke asiyefaa kitu, kwa kuwa katika wingi wa kuugua kwangu na kusikitika kwangu ndivyo nilivyonena hata sasa.” Eli akaridhika na kumwambia aende kwa amani, na Mungu wa Israeli amjalie haja aliyomwomba. Hana akashukuru, akaenda zake na kula na uso wake haukuwa na huzuni tena, kwani alijua BWANA atampatia mtoto. Watoto hasa wa kiume kwa wengi wasio na uvumilivu waliona mambo yataharibika wakikosa warithi na vijana wa kiume watakaowasaidia kwenye shuguli mbalimbali, kwani mtoto wa kike alikuwa sehemu ya jamii aliyoolewa. Basi Waliabudu asubuhi iliyofuata na mumewe Shilo, kisha wakaenda kwao Rama. Hana alipata mimba na kumzaa mtoto wakamwita Samweli, ikiwa ina maana, “nimemwomba Mungu.”

Wakakwea Shilo kila mwaka kwenda kutoa dhabihu, ila Hana hakwenda mpaka mtoto alipoachishwa kunyonya ili amlete kwa Bwana, na kukaa huko daima. Mama huyu alikuwa ni shujaa kwani kuachana na mtoto wake mdogo lilikuwa ni jambo kubwa. Elkana mumewe alimruhusu Hana afanye kama alivyokusudia moyoni mwake. Hana alikuwa na kazi kubwa ya kumfundisha mtoto mambo ya muhimu kabla ya kuachana kama vile mama wa Musa alivyofanya. Tena alijua kwamba watoto wa Eli ni wakorofi na waovu, na baba yao aliwaogopa kuwaambia Ukweli wa kuwasaidia, bali Hana hakutoa udhuru. Mtoto Samweli alipoachishwa kunyonya, wazazi walienda na sadaka ya ng’ombe watatu, unga na chupa ya divai. Naye Samweli alikuwa mtoto mdogo, nao wakatoa ile dhabihu ya kuteketezwa. Hana akamwambia Eli kwamba yeye ndiye alikuwa yule mwanamke ambaye alifikiria ni mlevi alipomsihi BWANA kwa uchungu ili ampatie mtoto, akasema “naliomba nipewe mtoto huyu, BWANA akanipa dua yangu niliyomwomba. Kwa sababu hiyo mimi nami nimempa BWANA mtoto huyu; wakati wote atakaokuwa hai amepewa BWANA. Naye akamwabudu BWANA huko.” Hana akaimba wimbo akasema “moyo wangu wamshangilia BWANA, pembe yangu imetukuka katika BWANA, kinywa changu kimepanuka juu ya adui zangu; kwa kuwa naufurahia wokovu Wako, hakuna Aliye Mtakatifu kama BWANA… Wala hakuna mwamba kama Mungu wetu…aliyekuwa tasa amezaa watoto saba...BWANA hufukarisha mtu, tena hutajirisha; hushusha chini, tena huinua juu. Humwinua mnyonge toka mavumbini, humpandisha mhitaji kutoka jaani… kwa maana nguzo za dunia zina BWANA, Naye ameuweka ulimwengu juu Yake. Yeye atailindia miguu ya watakatifu Wake;… washindanao na BWANA watapondwa kabisa.” Tupo safarini, tunapita hapa duniani ambapo ni nchi ya adui mkubwa wa Mungu, hebu tumlilie Mungu kama Yakobo kwa tukishikamana Naye tukisema “sitakuacha eh Bwana, mpaka unibariki”. Hivyo ndivyo Mungu wetu alivyo. Yeye Yuko tayari kusikia maneno ya

mioyo yetu yenye huzuni. Iwe jibu la sala yako ni ndiyo, hapana au subiri kidogo, unaweza kuwa na uhakika kabisa kwamba Mungu anasikia.

Tuna haja ya kujifunza kudai ahadi za Mungu kwenye Sala zetu. Hakuna mwanadamu aliyeweza kuelewa kile Hana alikuwa akipitia, ila Mungu tu Ndiye aliyejua. Yule anayeweka machozi yetu kwenye chupa anaelewa na kutusikia. Kila wakati tumimine mioyo yetu Kwake kwa sababu Yeye anajali. Hatuna haja ya kujibu kwa ujeri watu. Elkana aliharibu amani ya nyumbani mwake kama Abrahamu, wakati alipojaribu kutatua shida ya kutokuwa na watoto kwa kuoa mke wa pili. Labda alikuwa amechoka kungojea Mungu ajibu sala yake, na hivyo kukosa imani. Wakati wowote tunapotatua shida kwa njia ambayo Mungu haikubali kwa sababu tumechoka kumngojea Mungu, tunatengeneza shida kubwa zaidi. Kwa hivyo, wacha tumngojee Bwana, haijalishi inachukua muda gani. Hana alimwomba Bwana mwana, ili aweze kumrudishia tena... hii ni roho isiyo na ubinafsi. Unapopata machungu soma sala hii tena. Utayasikia maumivu yake moyoni hakika. Labda sala yako haikuwa ya mtoto kama yeye, lakini wakati sala inakwenda bila kujibiwa kisa kinaonyesha ni nini cha kufanya. Mwaliko unatolewa kuendelea kusali. Hana alionekana mbele ya Bwana Hekaluni na akaomba kwa moyo wake wote, na hisia nyingi bila kutamka maneno, yaani maneno yalikataa kutoka, nayo yakakaa ndani! Hana alijisahau akiomba, akajiona yupo mbele za Mungu Mwenyewe! Mungu anaelewa na kusikia ombi letu. Hivyo ndivyo Mungu wetu alivyo. Yuko tayari kusikia roho zetu za huzuni. Ikiwa jibu la maombi yako ni ndio, hapana au subiri kwa muda, unaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu anasikia.

*Tunaweza Kumkaribia MUNGU kwa Ujasiri Kupitia Jina la Yesu—Unyenyekevu na ucha Mungu vinapaswa kubainisha tabia ya wote wanaokuja katika uwepo wa MUNGU. Kwa Jina la Yesu tunaweza kwenda mbele Zake kwa ujasiri, lakini hatupaswi kumkaribia kwa ujasiri wa kiburi ( au kudhania), kana kwamba Yupo ngazi moja na sisi. Kuna wale ambao wanazungumza na MUNGU mkuu na Mwenye nguvu zote na mtakatifu, ambaye anakaa katika nuru isiyoweza kufikiwa, kama wanavyoweza kuongea na mtu wanayelingana naye, au hata mtu duni kuliko wao. Kuna wale wanaotenda katika nyumba Yake Mungu kwa namna ambayo hawazezi kufanya katika chumba cha kuonania na mtawala wa kidunia. Hawa wanapaswa kukumbuka kuwa wako machoni Pake Yeye Yule ambaye maserafi humwabudu, mahali ambapo malaika hufunika nyuso zao mbele Yake.

---

Je, tunajifunza nini kuhusu kutunza nadhiri kama Hana? Kwa nini Hana aliimba? Kuhani mkuu aliitwa nani? Watu walihudhuria ibada na kutoa sadaka wapi? Je, ungekuwa na mtoto wa miaka 5 tu, ungemfundisha yapi kabla hajaondoka nyumbani mwako. Kwa nini Elkana alimwambia Hana asilie? Je, ungekuwa Penina ungebadilisha jambo gani? Kwa nini Eli alifikiri Hana alikuwa amekunywa pombe? Samweli ina maana gani? Je, wimbo wa Hana ulirudiwa tena na nani? Samweli alichukuliwa hekaluni akiwa na umri gani? Je, umebarikiwa na mama au baba ambaye anasali? Elezea! Kwanini mitara huleta huzuni?

**SIKU YA 72**
**(Machi 12)**

# Mtoto Samweli Akiwa Hekaluni

**– 1 Samweli 2-3**

Elkana na mke wake Hana walirudi nyumbani na yule mtoto Samweli akamtumikia Bwana mbele za Eli. Nafikiri Samweli alilia kuachana na mama yake, na mama pia alilia. Ila tunapoweka nadhiri zetu, tusifanye dhihaka kwa kutozitimiza. Mama huyu alimfanyia kanzu ndogo na kuileta akija kumwona mara moja kwa mwaka. Eli alimbariki Elkana na kumwambia Mungu ampe uzao mwingine kwa Hana. Naye alizaa watoto wa kiume watatu na wa kike wawili. Je, unamuona Samweli akikimbia kuwalaki baba na mama wakimtembelea? Samweli akakua mbele za BWANA na Mungu alikuwa pamoja naye. Uadilifu wa mtoto Samweli unalinganishwa na uovu wa wana wa Eli ambao walikuwa wakifanya kazi kama makuhani Hekaluni. Vijana hao wawili walawi walikuwa wakitumia nafasi zao kudanganya Wanaisraeli na kutekeleza miradi yao ya uovu. Walikuwa wakifanya mambo haya kwa sababu hawakumjua Mungu kibinafsi na hawakujali utakatifu wa majukumu yao.

Basi wana wa Eli walikuwa watu wasiofaa kitu, wasiomjali BWANA wala watu. Walipora sadaka za nyama zilizoletwa kwa kafara huko Shilo, kwa uroho wakala hata kabla ya huduma ya wakfu. Watu wakiwaambia kinachotakiwa kufanya walisema msipotupa au kuacha tufanye tunachotaka basi tutatwaa kwa nguvu. Hivyo dhambi yao ilikuwa kubwa sana machoni pa BWANA, kwa maana walidharau sadaka za BWANA na kulala na wanawake waliohudumu hekaluni kwa nguvu. Eli alikuwa mzee na alisikia juu ya vituko na dhambi za watoto wake waliohudumu hekaluni. Aliwauliza kwa nini wafanye uovu huu, na kuwakosesha watu kwa Bwana? Akasema, “mtu mmoja akimkosa mwenzake, Mungu atamhukumu; lakini mtu akimkosea Bwana ni nani atakayemtetea?” Lakini hawakuisikiliza sauti ya baba yao. Ni jambo la huzuni watoto kutosikiliza sauti ya mzazi na kuhani wa Mungu. Hatuelezwi mengi ila wazazi pia ni vyema watoe adhabu au nidhamu wakati watoto wakiwa wadogo. Kutii wazazi ni Amri ya tano ya BWANA, yenye ahadi ya kuishi miaka mingi. Mungu alikusudia kuwaadhibu, maana aliona hawana toba.



Samweli aliendelea kukua akipata kibali machoni pa BWANA na watu. Ni muhimu kupata kibali machoni pa Mungu na watu pia, maana watu wanakuona na kuishi na wewe kila siku. Wanachukua habari njema zako na kukubariki, na pia wanakuombea baraka. Mungu alimwambia Eli kwamba alichagua Walawi kumtumikia kwa kuhudumu hekaluni. “Kwa nini basi mnaipiga teke dhabihu Yangu na sadaka nilizoziamuru katika maskani Yangu; ukawaheshimu wanao kuliko Mimi, mpate kujinenepesha kwa sadaka zote za watu Wangu Israeli zilizo njema… wanaoniheshimu nitawaheshimu,

na wao wanaonidharau watahesabiwa kuwa si kitu." Kweli tukimheshimu Mungu Naye atatuheshimu. Mungu hapa alisema, "tuheshimiane!" Japo sisi ni wadogo anatuheshimu kama tukijiheshimu, si jambo la ajabu hilo? Basi Mungu alikusudia kuikata mbari ya baba yao kuwa kuhani. Akamwambia wazao wa nyumba yake watakufa, Nami "nitajiinulia kuhani mwaminifu, atakayefanya sawasawa na mambo yote Niliyo nayo katika Moyo Wangu, na katika nia Yangu; Nami nitamjengea nyumba imara; naye atakwenda mbele ya masihi Wangu milele" alisema haya akimaanisha hatimaye Kristo Ndiye atakuwa kuhani wa milele. Mungu akamwambia kwamba watoto wake Hofni na Finehasi wote watakufa siku moja.

Mtoto Samweli aliendelea kutumika kwa BWANA mbele ya Eli, na siku zile Neno la BWANA lilikuwa adimu, hapakuwa na mafunuo dhahiri. Siku moja Eli akiwa amelala usiku, macho yakiwa yameanza kupofuka hata asiweze kuona, taa ya hekalu ikiwa inawaka na Samweli alikuwa amelala katika moja ya vyumba vya hekalu, na akasikia sauti ikimuita, "Samweli, Samweli" naye akaitika "Mimi hapa," akafikiri ni Eli amemuita. Akaenda kwa Eli na kusema "mimi hapa, maana uliniita" au "naam". Eli akamwambia sikukuita, nenda kalale tena. Aliendа kulala na akaitwa mara ya pili tena, "Samweli, Samweli!" naye alienda tena kwa kuhani mkuu Eli, akiwa na uhakika sauti imemwita, na Eli akasema tena sikukuita mwanangu, nenda kalale tena. Samweli alikuwa bado hajui jinsi BWANA anavyowasiliana na mtu, na Neno la BWANA lilikuwa bado halijafunuliwa kwake kwa undani. BWANA alipomwita Samueli mara ya tatu, aliitika tena na kumwendea Eli, ndipo Eli alipogundua kuwa ni BWANA anayemwita mtoto. Japo yeye alikuwa na cheo cha kuhani mkuu na mtawala wa Israeli wa ngazi ya juu, Mungu alikuwa amemwacha, kwa sababu ya kutosimamia nyumba Yake vyema, na watoto wakawa wanamtawala. Basi alimwambia Samweli kwamba aende akalale na akisikia sauti tena aseme, "Nena BWANA, kwa kuwa mtumishi wako anasikia." Samweli alienda kulala na akaisikia sauti ile ikiita, akasema, 'Nena BWANA kwa kuwa mtumishi Wako anasikia, na BWANA akamwambia Samweli kwamba atatenda tendo katika Israeli na kila atakayesikia masikio yake yatamwasha. Akasema anaenda kutimiza ile adhabu ya uovu wa nyumba ya Eli, na kuhukumu nyumba yake milele "kwa kuwa wanawe walijiletea laana, wala yeye hakuwazuia." Akasema uovu wa nyumba ya Eli umekuwa mkubwa hata wakiungama na kutoa kafara haitasaidia. Walikuwa wamemkufuru Roho wa Mungu, kwa kuwa alikuwa akiwaambia "wajirudi" nao wakakataa kusikia, mpaka sauti hii ikatoweka. Mtu mmoja alisema kwamba upendo wa namna hii kwa watoto ni upendo feki. Kwani mioyo yao ilikufa ganzi na dhamira haikuwashtaki walipotenda uovu. Alipomaliza kupata ujumbe wa BWANA, Samweli alilala mpaka kesho yake, na akajaribu kuepuka kumwambia Eli yale aliyoambiwa na BWANA kwa hofu maana alikuwa mkuu wake. Hata haijulikani kama alipata usingizi vizuri, maana alimpenda Eli, na Eli alimpenda, alikuwa kama baba yake na hakupenda kumpa habari mbaya.

Basi Eli alimwita Samweli na kumwambia "Ni Neno gani alilosema nawe? Nakusihi, usinifiche". Samueli akamwambia maono aliyopata asimfiche Neno na Eli akasema, "BWANA na afanye alionalo kuwa ni jema." Samweli akakua na BWANA akawa pamoja naye, wala hakuliacha Neno Lake lianguke chini. Watu wakatambua kwamba

BWANA yupo na Samueli na kwamba sasa alikuwa ndiye nabii. Watu wakapata tumaini tena la wokovu. BWANA akaonekana tena Shilo, kupitia Samweli, na Neno la Mungu likawajia Israeli kupitia Samweli. Samweli akawa mwamuzi wa 15 wa Israeli, na wa mwisho. Mtu asidharau utoto wako au ujana wako, Mungu anaweza kukutumia wewe akaacha wazee wakubwa. Imesemwa, Afadhali fukara mwenye hekima, kuliko mzee mfalme mpumbavu au afadhali kijana maskini mwenye hekima kuliko mfalme mzee aliye mpumbavu. Jambo la Muhimu ni kusikiliza sauti ya Mungu na kutii Mapenzi Yake Naye atazungumza nawe, hata ukiwa mtoto mdogo. Tunaona Samweli alileta furaha kwa wengi kwa sababu alikubali mwito wa Mungu na kutenda kwa uaminifu. Mungu ana mpango na maisha yako. Je, hutamwomba Mungu akusaidie kumfuata na kujipa furaha wewe mwenyewe na wengine pia?

Inawezekana kumpa mtoto mafunzo au malezi mazuri nyumbani, na bado yeye akawa mwana mpotevu. Kwa mfano, Kaini na Abeli walilelewa na wazazi wale wale, lakini mmoja alikua muuaji, na mwingine mtoto mzuri wa Mungu. Baada ya kusema haya, tunajua kwamba mafunzo mazuri nyumbani ni sharti la kwanza katika kukuza tabia nzuri kwa watoto na vijana. Eli alihusika na kile watoto wake walichokitenda, na Hana alishiriki katika kukuza tabia nzuri ya Samweli. Yote ili yawe sawa, ukweli huu unashikilia: "Mfundishe au mlee mtoto katika njia impasayo kwenda, naye hataisahau au kuchepuka hata atakapokuwa mzee." Mithali 22:6. Eli alikataa kuwaadhibu watoto wake, naye alijipatia matokeo mabaya, Hana na Elkana walimfundisha Samweli njia anayopaswa kwenda, na hata ushawishi mbaya wa watoto wa Eli haukuweza kumpindisha, japo alikuwa mtoto mdogo. Wale ambao bado tunalea watoto tafadhali tulikumbuke hilo na kupiga magoti, tukiwaleta watoto wetu kwa Mungu kwa maombi! Mama na baba dhaifu, wakiwa magotini, ni nguvu tosha. Tuombeane katika safari hii, hasa katika ulimwengu wa utandawazi, simu, media, vyombo vya habari, televisheni, kompyuta n.k.

*MUNGU Ataliheshimu Jina la Yesu Katika Maombi yetu—Kila ahadi katika Neno la MUNGU hutupatia jambo la kuombea, ikiwasilisha Neno la Yehova aliloahidi kama uhakikisho wetu. Haijalishi baraka yoyote ya kiroho tunayoihitaji, tumependelewa kuidai kupitia Yesu. Tunaweza kumwambia Bwana, kwa unyenyekevu na usahili wa mtoto kile tunachohitaji haswa. Tunaweza kumwambia mambo yetu ya muda mfupi, tukamwomba mkate na mavazi na Mkate wa Uzima na joho la haki ya Kristo. Baba yako wa mbinguni anajua kuwa unahitaji vitu hivi vyote, na umealikwa kumuomba kuhusiana na hivi vyote. Ni kupitia Jina la Yesu kwamba kila neema inapokelewa. MUNGU ataheshimu Jina hilo, na atakidhi mahitaji yako kutoka katika utajiri wa ukarimu Wake (anatoa kwa uhuru mkubwa).

---

Samweli alivaa nguo gani? Mama ana ushawishi wa aina gani kwa mtoto wake? Mungu alimtokeaje Samweli? Kwa nini Mungu alimuacha Kuhani Eli? Je, watoto wa Eli walijilaanije? Je, Mungu anafanya kazi na watu wa umri gani? Kwa nini utii ni bora? Je, unafikiri baba na mama Samueli walifikirije walipoona mtoto wao amekuwa nabii? Kwanini Eli analaumiwa na watoto walikuwa watu wazima. Je, tunawezaje kuondoa unyanyapaa kwa wale ambao hawana watoto au ambao hawakuolewa? Kwanini ni vyema viongozi wa kiroho wawachukue vijana na kuwashauri na kuwafundisha kazi? Utaijuaje sauti ya Mungu anapokuita?

**SIKU YA 73**
**(Machi 13)**

# Wafilisti Wachukua Sanduku la Agano (Ikabodi)

**- 1 Samweli 4-7**



Wafilisti walikusanyika kupigana na Israeli na Waisraeli walitoka na kwenda vitani wakatua karibu na Ebenezeri. Wafilisti wakajipanga wapigane na Waisraeli 4000 walipigwa na kuuwawa na wafilisti 2000 tu. Ndipo Israeli wakasema, "Mbona BWANA ametupiga leo mbele ya Wafilisti?" Wakasemezana walilete Sanduku la BWANA toka Shilo, wakisema "lije kati yetu na kutuokoa katika mikono ya adui zetu." Wakaleta sanduku la BWANA wa majeshi, akaaye juu ya makerubi na Hofni na Finehasi wana wa Eli walikuwa huko pamoja na sanduku, na lilipoingia kambini watu walipiga kelele, na Wafilisti waliposikia walisema "ni mshindo wa kelele gani hizi kambini mwa Waebrania? Wakatambua kuwa sanduku limefika, wakaogopa na kusema, "Ole wetu! ni nani atakayetuokoa na mkono wa miungu hawa walio hodari?" Wakakumbuka kwamba Wamisri walipigwa na Mungu huyu jangwani. Wakajitia nguvu, wakawapiga Waisraeli na Waisraeli wakakimbia hemani mwao, wakauawa watu "thelathini elfu wenye kwenda vitani kwa miguu." Na sanduku la

BWANA likatwaliwa; na Hofni na Finehasi wakauawa siku moja. Mtu mmoja wa Benyamini alipiga mbio kwenda Shilo nguo zake zikiwa zimezaruliwa na mavumbi kichwani ili kupeleka habari mbaya kwa kuhani mkuu Eli. Alipofika alimkuta Eli amekaa kwenye kiti, moyo wake ukitetemeka, na mji wote ulikuwa unalia. Eli aliuliza kelele hizo zinatoka wapi? Mtu yule akamwambia Eli yaliyotokea. Eli aliyekuwa na miaka 98 na kipofu, aliposikia, na kwamba hata sanduku la Agano la Bwana limechukuliwa, alianguka kitini pake kwa nyuma, na shingo yake ikavunjika, maana alikuwa mzee tena mzito. Alikuwa amewaamua Israeli kwa miaka 40. Mke wa Finehasi alikuwa mjamzito, na aliposikia habari za sanduku kutwaliwa na kifo cha mumewe na baba mkwe, alipata uchungu na kuzaa mtoto, na kumwita jina lake Ikabodi, maana yake 'utukufu wa Mungu umeondoka katika Israeli' kwa vile sanduku la Agano la BWANA limechukuliwa.

Wafilisti walichukua sanduku la Agano la Mungu na kwenda nalo Ashdodi na kuliweka katika nyumba ya mungu wao aliyeitwa Dagoni, aliyekuwa na kichwa cha mtu na mkia wa samaki. Walipoamka asubuhi walikuta Dagoni ameanguka kifudifudi, mbele ya sanduku la Bwana. Wakaisimamisha ile sanamu ya Dagoni mahali pake lakini kesho yake wakakuta Dagoni ameanguka tena chini ya sanduku la BWANA na kichwa chake na vitanga vyake vya mikono vimekatika, vikiwa vimelala kizingitini, na kiwiliwili tu ndio kimebakia. Mkono wa Bwana ukawa mzito kwa watu wa Ashdodi akawapiga watu hawa kwa majipu makali. Watu hawa wakaapa kwamba hili sanduku halitakaa kwao maana mkono Wake ni mzito juu yao na juu ya mungu wao. Walituma viongozi wao waende kuuliza, "tulifanyeje sanduku la Mungu wa Israeli?" Wakajibu sanduku lihamishiwe Gathi. Walilihamisha na mkono wa Bwana ukawa juu ya Gathi nao wakapigwa na kufadhaishwa sana. Watu wote, wakubwa kwa wadogo, wa mjini au wa mashambani wakapata majipu. Wakalituma sanduku kwenda Ekroni na lilipofika watu wa Ekroni walifanya kelele wakisema, "wamelileta hilo sanduku la Mungu wa Israeli kwetu, hata kutuua sisi na watu wetu." Wakatuma wajumbe waliondoe hilo sanduku, kwa sababu fadhaa ilizidi, na mkono wa Bwana ulikuwa mzito mno huko kwani wale wasiokufa, walipigwa na majipu. Kilio cha mji kikafika mbinguni.

Sanduku la Agano la BWANA lilikuwa kwa Wafilisti kwa miezi saba. Wakaleta makuhani wao na waaguzi wakitaka kujua wafanyeje kuondokana na 'janga hili'. Basi wakuu wakaamua walirudishe Sanduku la Agano, na lisiende tupu bali watoe matoleo ya sadaka ya kuomba msamaha kwa kosa lao ndipo watapona na kufunguliwa shida zao. Walipeleka na kutoa "majipu ya dhahabu matano, na panya wa dhahabu watano." Tano ikisimamia miji yao mitano. Wakaamrishwa kumtukuza huyo Mungu wa Israeli, "huenda ataupunguza uzito wa mkono Wake juu yenu, na juu ya miungu yenu, na juu ya nchi yenu." Basi wakaambiwa wafanye gari jipya na ng'ombe wanaonyonyesha wakilipeleka lile Sanduku la zawadi, bila kujali ndama wao zizini, na hivyo watajua wamepata kibali mbele ya Mungu wa Israeli. Basi ng'ombe walishika njia moja kwa moja kwenda huku wakilia nao wakafika Israeli na kukuta wanavuna ngano bondeni. Watu wakafurahi kuona Sanduku la Agano la BWANA likija, na gari likatua kwenye konde la Yoshua na kusimama. Wakapasua miti ya lile gari, wakawatoa ng'ombe kuwa sadaka ya kuteketezwa. Walawi wakashusha lile Sanduku na vile vitu vya dhahabu na kutoa sadaka za kuchinja na kuteketezwa,

na wale viongozi wa Wafilisti walirejea Ekroni. Jambo la ajabu ni kwamba, wana wa Israeli wa Beth-shemeshi lilipofika sanduku wakakosa kicho na kulifungua sanduku la BWANA, ili wachungulie na kuona kilichomo wakati ambapo hawakuruhusiwa hata kuligusa isipokuwa makuhani tu. Wakafa watu wapatao 50,070! Hata leo tunapaswa kuwa na adabu nyumbani mwa BWANA. Tusipige kelele au kutembea hovyo ovyo au kukimbia. Watu wakalalamika kwa pigo hili na kusema, "Ni nani awezaye kusimama mbele za BWANA, Huyu Mungu Mtakatifu?" Wakatuma wenyeji, watu wa Kiriath-yearimu waje walichukue sandulu la agano. Wakalichukua na kulileta kwenye nyumba ya Abinadabu, nao wakamtenga mwanawe Eleazari alilinde sanduku hili. Sanduku lilikaa pale kwa miaka 20 kwani Kuhani alikuwa amekufa. Baada ya miaka hiyo, Waisraeli wakaomboleza mbele za BWANA. Naye Samweli akawaambia watu, "ikiwa mnamrudia BWANA kwa kwa mioyo yenu yote, basi, iondoleeni mbali miungu migeni" na kumtengenezea BWANA mioyo yenu, mkamtumikie Yeye peke Yake, Naye atawaokoa katika mikono ya Wafilisti. Ndipo Waisraeli wakaondoa miungu ya Baali, Ashthorethi, na kumtumikia BWANA peke Yake.

Japo Waisraeli walikuwa watu wa Mungu, mfano wao ulikuwa mbaya. Majirani zao wangemkubali Mungu wao kirahisi, na kuacha miungu yao, lakini kwa sababu ya dhambi walikuwa watumwa wao na wakafikiri miungu yao ni bora zaidi. Walipata ishara nyingi ila walikuwa wagumu kuamini, nasi pia tuna udhaifu huo, tuombe Mungu atusaidie. Tunahuzunika tunapoona ufisadi katika serikali zetu, lakini tunahuzunika zaidi tunapoona ufisadi kanisani. Lazima tuongozwe na Roho ili tujue mafanikio halisi ni kumtegemea Mungu, kumwamini, kumpenda na kumtii. Yusufu na Yohana wote walitoka gerezani; Yusufu akaenda Ikulu, Yohana akaenda Kaburini. Kwa mtazamo wa haraka, Yohana hakuwa na mafanikio. Lakini kutokana na utume wake (Mtangulizi wa masihi) baada ya ya kufanya kazi ya kumfunua masihi, hakika Yohana alikuwa amefanikiwa. Mafanikio ya muhimu sana kwa watu wa Mungu ni kumfanya Mungu kuwa wa kwanza. Hitaji kuu la ulimwengu ni hitaji la watu-watu ambao hawatanunuliwa wala kuuzwa, watu ambao ndani kabisa ya nia zao ni wakweli na waaminifu, watu wasiogopa kuiita dhambi kwa jina lake halali na halisi, watu ambao dhamiri zao ni aminifu katika wajibu kama ilivyo ncha ya dira ya kaskazini, watu watakaosimama kwa ajili ya haki japo mbingu zianguke. Wakati Israeli kama taifa lilishindwa kumfuata Mungu na kumpenda kwa mioyo yao yote, leo tunaletewa tena kwenye mtihani huo-huo. Tunapoushinda, mbingu inatuita, watu waliofanikiwa.

Kusikia sauti ya Mungu ni kama kujifunza lugha mpya; ni lazima tufanye kila kitu katika kuwa makini ili tujifunze na kutofautisha kile ambacho ni sauti ya Mungu na ambacho sicho. Roho Mtakatifu ni msemaji wa Mungu. Mungu anazungumza nasi kwa njia ya Roho Mtakatifu (Yohana 16:13) "Lakini Yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza ninyi katika kweli yote……" Mungu anaongea leo! Leo, ikiwa tutaisikia sauti Yake, tusiifanye migumu mioyo yenu. . . ." Waebrania 3:7-8 Samweli aliwaletea wengi furaha kwa sababu alikubali mwito wa Mungu na kutenda kwa uaminifu. Mungu ana mpango na maisha yako leo. Je, hutamwomba Mungu akusaidie kumfuata na kujipa furaha wewe mwenyewe na kisha wengine? Samweli alijitoa kwa huduma na utume na alipata kibali kwa Mungu na wanadamu.

Vijana tunapaswa kujifunza kumfuata Mungu na kumtumikia kwa uaminifu. Nasi wachungaji, wazee na maafisa wa kanisa, tunaweza kuwa na bidii sana kushugulikia kazi ya Mungu na tukapuuza familia zetu wenyewe. Tunaweza kuendesha kanisa kwa mafanikio na kudhihirisha utakatifu, wakati nyumba zetu haziko katika mpangilio. Kwa sababu hiyo Paulo akizungumzia wazee katika kanisa anasema "yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje Kanisa la Mungu?" Ayubu alikuwa kielelezo cha baba ambaye aliwaombea wanawe ikiwa wamefanya dhambi bila kujua (Ayubu 1:5). Lakini hakuwezi kuwa na upatanisho wa dhambi ya makusudi.

*Hatupaswi kuomba tu katika Jina la Kristo, bali kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hii inaelezea kuwa ina maana gani kusema, "Roho Mwenyewe hutuombea kwa kuugua na maumivu yasiyoweza kutamkika." Warumi 8:26 MUNGU hufurahia kujibu maombi kama hayo. Tunapotoa ombi katika Jina la Kristo kwa dhati na nguvu, kuna ahadi yenye nguvu kutoka kwa MUNGU kwamba Yu karibu kujibu ombi letu "kwa wingi zaidi ya yote tunayoomba au kufikiri." Waefeso 3:20.

---

Nini maana ya Ikabodi? Kosa la Eli lilikuwa nini? Eli alikufaje? Kwa nini Wafilisti walipigwa na majipu? Kwa nini watu 50,070 walikufa? Kwa nini si vizuri kuzungumza-zungumza kanisani na kucheza? Watu walipomjia Samweli kumrudia BWANA aliwaambiaje? Je, kwanini ni vibaya kuwaendekeza au kuwadekesha watoto?

**SIKU YA 74**
**(Machi 14)**

# Samweli, Mwamuzi wa Mwisho wa Israeli

**- 1 Samweli 7-9**



Wakati sanduku la Agano limechukuliwa, Samueli alikuwa mtoto bado. Baada ya miaka kadha wa kadha Samweli Walipomwendea Samweli na kuondoa miungu yao, Samweli alisema "wakusanyeni Israeli yote Mispa, nami nitawaombea ninyi kwa Bwana." Waisraeli wakakusanyika Mispa na wakateka maji na kuyamimina mbele za BWANA na wakafunga na kusema "Tumemfanyia Bwana dhambi." Samweli akawaamua watu Mispa, na Wafilisti waliposikia Waisraeli wamekusanyika Mispa walipanda kupigana nao, na Waisraeli walipoona hivyo wakaenda kwa Samweli na kumwambia, "Usiache kumlilia, Mungu wetu, kwa ajili yetu, kwamba atuokoe "mikononi mwa Wafilisti. Samweli akatoa sadaka ya kuteketezwa kwa BWANA, na Wafilisti walipokaribia BWANA akawapiga kwa ngurumo mshindo mkubwa sana, na kuwafadhaisha, wakaangamizwa mbele ya Israeli. Wakatoka Mispa na kuwafukuza Wafilisi na kuwapiga. Samweli akatwaa jiwe na kulisimamisha, kama bango, naye akaliita Eben-ezeri maana yake "BWANA AMETUSAIDIA." Wafilisti walishindwa wasiingie tena kwenye mipaka ya Israeli siku zote za Samweli, kukawa na amani. Samweli akawaamua Israeli maisha yake yote, naye alienda

akizunguka Betheli, Gilgali, na Mispa kuamua na kurudi kwake Rama, akamjengea Bwana madhabahu huko.

Samweli alipokuwa mzee aliwaweka wanawe kuwa waamuzi juu ya Israeli, mwana wake wa kwanza aliitwa Yoeli, wa pili Abiya. Ila wanawe hawakuenda katika njia zake na wakawa kama wana wa Eli, waliokuwa watumishi wa mshahara, wa kutaka kupata faida zao, na wakapokea rushwa na kupotosha hukumu. Ni msiba ulioje kuona wana wa Samweli wakikengeuka kwa kupata faida isiyo ya haki na kupokea rushwa na kupotosha haki. Hebu tuwaombee viongozi wetu wa kanisa leo, ili waweze kutembea daima kwa unyofu na uadilifu. Na kwa neema ya Mungu, na tuache daima tabia potovu na kuishi kwa kumheshimu BWANA, Mungu wetu.

Basi wazee wa Israeli walikutana Rama na kumwambia Samueli, "Angalia, wewe umekuwa mzee na wanao hawaendi katika njia zako, basi tufanyie mfalme atuamue, mfano wa mataifa yote." Samweli alikuwa na uchungu sana na neno hili, maana BWANA Ndiye alikuwa mfalme wao, na sasa wanataka kufanana na mataifa mengine. Samweli akamwomba BWANA, Naye BWANA akamwambia aisikilize sauti ya watu, "maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa Mimi." Hawanitaki Mimi BWANA Niwe mfalme wao. Japo Mungu aliwatendea makubwa toka Misri, bali walitaka kumwacha na kutumikia miungu mingine. BWANA akamwambia Samweli awaonye sana, na kuwaonesha jinsi mfalme atakavyokuwa sindano ya kuwanyanyasa. Samweli aliwapa ujumbe na kuwaambia kwamba mfalme atawafanya wao kuwa watumishi kwenye magari yake, watakuwa wapanda farasi, watapiga mbio mbele ya magari yake. Watakuwa maakida wake, na atawaweka walime mashamba yake, na kuvuna, na kufanyiza zana za vita. Binti zao watachukuliwa kutengeneza manukato, watafanywa wapishi, na mfalme atachukua mashamba yenye mazao mazuri ili awape watumishi wake. Mfalme atawatoza ushuru wa mbegu zao za mazao, awape watumishi wake na atawatwaa wao kuwa watumishi na wajakazi. Atachukua ngombe wao wazuri na punda wao wazuri awatumie kwa kazi zake binafsi. Mfalme atawatoza fungu la kumi na la makundi yao nao watakuwa watumwa wake. Mungu akawatahadharisha kwamba watalia siku moja kwa sababu ya kujichagulia mfalme, naye hatawajibu. Watu hawa wakakataa kusikiliza sauti ya Samweli, wakakazana wanataka mfalme, ili wafanane na mataifa yote na kwamba mfalme angewaamua na kutoka nao kwenda kupigana vita. Samweli alikuwa anafanya kazi ya kuwaamua tayari, ila walikazana kutaka waliyokatazwa. Samweli alipeleka mambo yote kwa Bwana. Naye Mungu akamwambia tena Samweli aisikilize sauti yao, na awafanyie mfalme na akawaambia Israeli waende majumbani mwao.

Mungu hawaachi watoto Wake wanapofanya a uamuzi ambao sio bora. Hii ni kwa sababu upendo Wake hauna masharti na ni wa milele. Katika upotofu wetu, Mungu bado atatoa ushauri wa jinsi ya kuleta matokeo bora zaidi. Kwa hivyo, kwa mfano, ikiwa kazi uliyoichagua inaweza isiwe bora anavyotaka Mungu kwako, bado, ikiwa utamsikiliza na kumtii Yeye, atakuletea kile kilicho bora zaidi katika hali hiyo. Hii ni kwa sababu, ijapokuwa hukwenda kwa lile alilokuwa nalo kama bora kwako, bado Yeye anakupenda Naye hatakuacha kamwe. Huu ni upendo ambao hautakuachilia uende!

Katika kabila la Benyamini kulikuwa na mtu aitwaye Sauli mwana wa Kishi, naye alikuwa kijana mwenye uzuri na mrefu. Hakuwako mtu mzuri kuliko yeye; tangu mabega yake kwenda juu, alikuwa mrefu kuliko watu wote. Punda za baba yake Kishi walikuwa wamepotea, na babaye akamwambia aende kwa nabii au mtazamaji Samweli asaidiwe kujua punda walipoenda. Sauli alitwaa mtumishi na kwenda kuwafuata punda, walitafuta kwa muda naye akamwambia mtumishi warudi, maana baba yake ataanza kuona hofu juu yao kupotea zaidi ya punda kupotea. Lakini mtumishi alisema kwamba katika mji huu pana mtu wa Mungu (mwonaji) anaishi hapo; nayo asemayo hutokea, hivyo waende kwake awaambie habari ya punda. Sauli akauliza wampelekee mtu huyu zawadi gani? Ndipo mtumishi akasema ana robo shekeli, basi wakaenda kwa mtu wa Mungu. Walipofika mjini, wakakuta wasichana wanatoka kuteka maji, na wakawauliza kama wamemwona mwonaji, wakawaambia wafanye hima kwani ndiyo tu amekuja na yuko tayari kutoa dhabihu, na waende kabla ya hii shughuli kuanza. Walipokuwa wakiingia mjini, Samweli akawatokea kwenda mahali pa juu. BWANA alikuwa amemfunulia Samweli, jana yake kwamba, "kesho wakati kama huu, nitakuletea mtu kutoka nchi ya Benyamini, nawe mtie mafuta ili awe mkuu juu ya watu Wangu Israeli. Naye atawaokoa watu Wangu kutoka katika mikono ya Wafilisti. Hivyo samweli alipomwona Sauli, BWANA akamwambia huyu ndiye, niliyekwambia habari zake atakayewamiliki watu Wangu. Sauli alimkaribia Samweli akiomba, "tafadhali, uniambie nyumba ya mwonaji iko wapi?" Samweli alimwambia, yeye ndiye mwonaji, na aje naye juu, na kula pamoja naye na asubuhi angemwachia aende zake, kisha atamwambia yote "aliyo nayo moyoni mwake. Na wale punda zako waliopotea siku hizi tatu, usijiudhi kwa ajili yao; maana wameonekana, na yote yaliyotamanika katika Israeli amewekewa nani? Si wewe na nyumba yote ya baba yako? Sauli alishangaa kwamba yeye Mbenyamini, mtu wa kabila dogo, na ukoo mdogo kwa nini anamwambia vile?

Lutu alitaka nchi ya fanaka ya Sodoma, licha ya uovu wake, na alipoteza mali yake yote na wengi wa familia yake. Hapa Wanaisraeli wanasema "Tunataka mfalme!" Mara nyingi watu huogopa kutenda haki wakisema-Sitaki kumkasirisha rafiki yangu, Sitaki kupoteza kazi yangu nzuri, Kanisa langu litakua, Mtu mmoja dhidi ya umati hataleta tofauti, Nataka pesa zaidi, nguvu, na umaarufu nk. Haijalishi kisingizio, ikiwa Mungu amesema ana mpango kwetu, hakuna tunachofanya kitakachoboresha Hekima Yake. Ikiwa tunasisitiza njia zetu wenyewe, msimu wa giza la maisha upo mbele yetu. Hatuwezi kuwa watu wa kipekee wa Mungu na kufuata njia za ulimwengu. Mazoea yetu ya kula na kuvaa, mfumo wetu wa elimu na huduma za tiba zinapaswa kuendana na mapenzi ya Mungu. Hata utumiaji wetu wa mfumo wa mahakama unatakiwa kuendana na matakwa ya Mungu na sio jinsi ulimwengu unavyotenda. Wakati mwingine tunaogopa kuitwa washupavu na wenye misimamo mikali ikiwa tutafuata ile njia nyembamba ya Mungu. Je, tunapendezwa zaidi na kile ambacho wengine wanafikiri kutuhusu kuliko kufuata kile ambacho Mungu anataka kwa ajili yetu? Israeli walikuwa na fursa ya kuonyesha ukuu wa serikali ya Mungu, lakini badala yake walitaka kufanana zaidi na mataifa yaliyowazunguka. Walikuwa wanatafuta mfalme kama wapagani wote waliokuwa karibu nao. Hata nasi Tunatamani kuwa salama, kulindwa kutokana na misukosuko na uharibifu. Tunatamani kuwa salama kifedha, tukiwa na mali nyingi katika eneo linalofaa kwa kustaafu. Kuwa salama katika kazi zetu, nafasi zetu na ushawishi

juu ya wengine, kuheshimiwa na kujulikana. Kuwa salama katika afya zetu, na kuwa madaktari bingwa na sahihi,  na kula chakula bora. Kuwa salama katika mahusiano yetu, urafiki wetu, ndoa, watoto, familia na orodha inaendelea. Jibu la kawaida tunapohisi kutokuwa salama ni kutazama kila mtu anachofanya, na kile alichonacho, na kujaribu kuiga au kutamani. Tunaangalia kote kile ambacho kila mtu anacho au anachoonekana kuwa nacho, na kusema, "Nataka walicho nacho. Hivyo ndivyo vitanisaidia mimi kuwa salama. Tunachohitaji ni Yesu Kristo kuwa Mfalme mioyoni mwetu. Kuutafuta Ufalme Wake na haki Yake kwanza, na vitu vingine vyote tutazidishiwa.

*Kristo amesema, "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. Marko 11:24. "Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Yohana 14:13. Naye Yohana mpendwa, chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, anena kwa uwazi na uhakikisho ulio mkuu: "Tukiomba chochote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye hutusikia; na ikiwa tunajua kwamba Yeye hutusikia, lo ote tuombalo, tunajua kwamba tuna maombi ambayo tulimwomba."" 1 Yohana 5:14, 15. Basi  wasilisha maombi yako kwa ujasiri na msukumo kwa Baba katika Jina la Yesu. MUNGU ataliheshimu Jina hilo.

---

Samweli aliamua miji gani? Kwanini ni vibaya kucheza na vitu vitakatifu? Kwanini Mungu hawezi kulinganishwa na chochote? Kwa nini wana wa Israeli walitaka mfalme? Kwa nini Sauli alishangaa maneno ya Samweli? Kwa nini Samweli hakulaumiwa kwa tabia ya watoto wake? Nini maana ya Eben-ezeri? Taja majina ya wana wa Samueli.

**SIKU YA 75**
**(Machi 15)**

# Sauli Atiwa Mafuta Kuwa Mfalme

**- 1 Samweli 9-12**



Basi Samweli akamtwaa Sauli na mtumishi wake na kuwaketisha mahali pa heshima na watu walioalikwa kama thelathini hivi. Akamuita mpishi alete vinono vile alivyowekewa akiba, basi mpishi akatwaa paja la nyama na Samweli akasema kwa Sauli, "umewekewa hiyo wewe hata wakati uliokusudiwa." Sauli akala pamoja na Samweli kwa kushangaa, kisha wakashuka mahali pa juu na kufika mjini. Baadaye wakalala darini na kuongea, na ilipofika alfariji alimwita Sauli na kumwambia ainuke ampeleke kwao. Sauli aliinuka na wakatoka wawili, na waliposhuka mwisho wa mji, akamwambia Sauli amwambie mtumishi atangulie naye amwambie Neno la Mungu. Akatwaa chupa ya mafuta ya mizeituni na kuyamimina kichwani pake, kisha alimbusu akimwambia, "BWANA" amekutia mafuta au amemtawaza awe mfalme wa Israeli ili awaokoe mikononi mwa adui zao Wafilisti. Samweli akamwambia mambo fulani ili kuonesha kuwa hayo anayomwambia yalitoka kwa BWANA. Alimwambia kwamba akitoka kwake atakutana na wanaume wawili karibu na kaburi la Raheli, nao watakuambia punda uliokuwa unawatafuta wameonekana na baba yako ameacha kufikiri mambo ya punda bali anafikiri habari zenu akisema, "nifanye nini kwa ajili ya mwanangu?" Akamwambia akitoka hapo atakutana na watu watatu wanaokwenda Betheli, mmoja ana mwanambuzi, mwingine ana mikate mitatu na wa mwisho ana kiriba cha divai. Watakusalimu na kukupa mikate miwili, nayo utaipokea. Na utakapoenda Gibea utakutana na kundi la manabii wakishuka na watakuwa wakitabiri wakiwa na kinanda, kinubi na filimbi. Akamwambia atelemke Gilgali ili kutoa sadaka za kuteketezwa na amani, na kuongoja siku saba, naye Samweli atakuja kumwonesha yatakayompasa kuyafanya. Sauli aliondoka na kumwacha Samweli na Mungu akambadilisha moyo, nazo ishara zile zikatukia. Basi alipokutana na kikosi cha manabii; Roho wa BWANA akamjia naye akatabiri kati yao. Wote waliomjua zamani walishangaa na kusema, "ni nini lililompata mwana wa Kishi? Je, Sauli pia yumo miongoni mwa manabii?

Baba mdogo wa Sauli alimwuliza kwamba aliendа wapi, akamwambia yote yaliyotokea, isipokuwa yale ya 'kuwa mfalme.' Samweli alikusanya watu mbele za BWANA kule Mispa na kuwaambia BWANA wa Israeli asema aliwatoa Israeli kutoka Misri na kuwaokoa lakini leo "mmemkataa Mungu wenu, Naye Ndiye awaponyaye katika misiba yenu yote na shida zenu; nanyi mmemwambia sivyo, lakini weka mfalme juu yetu." Basi akawaambia waje wahudhurie mbele za BWANA makabila yote. Samweli alipowaleta wote, alitwaa kabila la Benyamini, na jamaa zao na kisha mtu kwa mtu, na Sauli mwana wa Kishi alitwaliwa jina lake, ila walipomtafuta hakuonekana. Walipoendelea kumwuliza BWANA, Naye BWANA akawajibu, "Tazama amejificha penye mizigo." Basi wakaenda mbio wakamleta kutoka huko, naye aliposimama kati ya watu, alikuwa mrefu kuliko watu wote, tangu mabega yake kwenda juu. Samweli akawaambia watu wote, mnamwona mtu huyu aliyechaguliwa na BWANA, ya kuwa hakuna mfano wake katika watu wote. Watu wakapiga kelele "Mfalme aishi!" Watu wengi wanaangalia sura na urefu, na si tabia na moyo wa kumpenda Mungu. Basi Samweli akawaambia watu madaraka ya mfalme; akayaandika katika kitabu na kukiweka mbele za BWANA na akawaruhusu watu wote waende nyumbani kwao. Samweli akaenda Gibea na kikosi cha watu, walioguswa mioyo yao na Mungu, ila wengine watu wasiofaa kitu walisema, "Huyu je, atatuokoaje? Nao wakamdharau, wasimletee zawadi," ila Sauli hakujibu kitu.

Sauli akasikia kilio cha watu wa Yabesh-Gileadi baada ya Waamoni kuwatokea. Waisraeli wakasema, "fanya mapatano nasi na sisi tutakutumikia." Sauli alipopata habari, akajiwa na roho ya Mungu kwa nguvu, na hasira zake zikawaka, naye akatwaa jozi ya ng'ombe na kukatakata vipande vyake, kisha akapeleka vipande mipakani mwote mwa Israeli kwa mikono ya wajumbe na kusema, "Yeyote asiyetoka nyuma ya Sauli na Samweli, ng'ombe zake watatendwa vivi hivi." Utisho wa BWANA ukawaangukia wale watu na wakatoka na kwenda huko, tayari kwa vita. Walipohesabiwa walikutwa ni 330,000. Wakatuma ujumbe kwa watu wa Yabesh-Gileadi kwamba kesho watakuja wakati wa jua kali, kuwapelekea wokovu. Sauli akapata vikosi vitatu na wakaingia kuwapiga Waamoni hata wakati wa jua kali, waliosalia walitawanyika hata wasiachwe wawili wao pamoja. Waliposhinda kwa uongozi wa Sauli, walimwendea Sauli awaue watu waliosema, "Je, huyo Sauli atatutawala?" Lakini Sauli akasema hakuna mtu atakayeuawa leo, maana leo BWANA amefanya wokovu katika Israeli. Basi Samweli akawaambia watu waende Gilgali ili waimarishe ufalme wa Sauli huko, kisha wakamtawaza Sauli mbele za BWANA na kuchinja sadaka za amani mbele za BWANA. Sauli na watu wote wakafurahi.

Samweli akawaambia watu wote wa Israeli kwamba amesikiliza matakwa yao na kumtawaza mfalme. Akasema, "Nipo hapa; basi, mnishuhudie mbele za BWANA, na mbele ya masihi Wake, nalitwaa ngombe wa nani? Au nilitwaa punda wa nani? Au ni nani niliyemdhulumu? Ni nani niliyemwonea au kupokea rushwa nipofushe macho." Watu wakajibu kwamba hakuwadhulumu, wala kuwaonea au kupokea rushwa. Naye akasema BWANA ni shahidi. Samweli akasimama kuhutubu matendo ya haki ya BWANA aliyowatendea baba zao. Kuanzia Yakobo, mpaka kuvuka shamu, na visa vya waamuzi. Akasema kwamba baba zao walipenda kuwatumikia Mabaali na Maashtorethi lakini hawakuwasaidia na adui zao. Akawaambia wamtazame

mfalme waliyemtaka na kumchagua. “BWANA ameweka mfalme juu yenu. Kama mkimcha BWANA, na kumtumikia, na kuisikia sauti Yake, msiiasi Amri ya BWANA, tena kama ninyi, na mfalme anayewatawala mkimfuata BWANA, Mungu wenu, mtapata mema. Bali msiposikia sauti ya BWANA, mkiiasi Amri ya BWANA, ndipo mkono wa BWANA utakuwa juu yenu, kama ulivyokuwa juu ya baba zenu. Basi Samweli akamwomba BWANA alete mvua kali ya ngurumo kwa ajili ya uovu wao mwingi walioufanya machoni pa BWANA wa kujitakia mfalme. Watu wakatetemeka wakisema, ‘Utuombee sisi watumwa wako kwa BWANA Mungu wako tusije tukafa, maana tumeongeza dhambi zetu zote kwa uovu huu, wa kujitakia mfalme.” Samweli akawaambia wasiogope, kwamba ni kweli wametenda uovu ila wamtumikie BWANA kwa mioyo yote yao, wala wasigeuke kufuata ubatili huo, wasifuate visivyoweza kuwasaidia au kuokoa kwa kuwa havifai kitu. BWANA hataacha watu Wake kwa ajili ya jina Lake kuu kwa kuwa imempendeza BWANA kuwafanya ninyi watu Wake mwenyewe. Samweli aliendelea kuwaombea na kusema, “Walakini mimi, hasha! Nisimtende BWANA dhambi kwa kuacha kuwaombea ninyi lakini nitawaelimisha katika njia iliyo njema na kunyoka. Mcheni BWANA tu, mkamtumikie kwa kweli na kwa mioyo yenu yote; maana, kumbukeni jinsi alivyowatendea makuu. Lakini kama mkiendelea kutenda mabaya, mtaangamia ninyi na ufalme wenu pia. Samweli akaandika sheria kwa mfalme na watu kutii kwenye kitabu, akarudi kwake.”

Sote tu napaswa kujiandaa kwa ajili ya kile ambacho kitatokea hivi karibuni katika ulimwengu na kuleta mshangao mkubwa. Maandalizi haya yanapaswa kufanya kwa kujifunza Neno la Mungu kwa bidii, na kujitahidi kupatanisha maisha yetu na kanuni Zake Mungu. Tunahitaji uamsho na matengenezo. Uamsho wa utauwa wa kweli miongoni mwetu ndilo hitaji kuu na la dharura zaidi kati ya mahitaji yetu yote. Kutafuta huu kunapaswa kuwa kazi yetu ya kwanza. Wakati umefika wa matengenezo ya kina kufanyika. Matengenezo haya yanapoanza, roho ya maombi itachochea kila mwamini, na roho ya mafarakano na ugomvi kanisani. “Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa Jina Langu, watajinyenyekeza, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi zao na kuiponya nchi yao.” 2 Mambo ya Nyakati 7:14. Daima Mungu Yu tayari kutimiza ahadi hii, ikiwa watu Wake watatimiza masharti ya ahadi hiyo. Aliweka ahadi hii kwa Israeli, Naye ataitunza kwa ajili ya kanisa leo. Je, hatujateseka vya kutosha chini ya utawala wa Shetani? Tuungame dhambi zetu, tuache “sanamu” zetu na tumwombe Mungu atukomboe kutoka kwa ufalme huu wa Shetani kwa kumtuma Yesu aje kutuchukua nyumbani. Hebu tusiabudu kama watu wengine, kwa kufuata njia za ulimwengu ili tukubaliwe. “Bali sisi ni wazao wateule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu; tupate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyetuita tutoke gizani tukaingie katika nuru Yake ya ajabu,” 1Petro 2:9. Wakati tunapoondoa upekee wetu wa imani, basi hatuna ujumbe wa kutoa kwa ulimwengu huu unaoangamia!

Udunia ni kumkataa na kumwasi Mungu. Ugumu wa mioyo ni kukataa mwito wa kuwapenda jirani zetu kama sisi wenyewe, na hivyo kutomtii Mungu. Hoja yenye nguvu zaidi kuhusu Ukristo ni Mkristo mwenye upendo na anayependeka. Hakuna kitu kinachouweka wazi Ukristo kama lawama za maadui zake kuhusu udunia na

ugumu wa mioyo ya wale wanaoukiri. Wafuasi wote wa Kristo wanapaswa kuwa waangalifu, wasije wakaleta lawama kwa dini yao. Gandhi kiongozi wa India alisema, "Kama si Wakristo, ningekuliwa Mkristo." Ingawa hoja ya Gandhi si sahihi, Kristo amesema tuna jukumu zito la kuwasaidia watu kumjua na kwamba sisi ni wanafunzi Wake (Yohana 13:34-35).

* Katika kila familia inapaswa kuwe na wakati uliowekwa wa ibada ya asubuhi na jioni. Inafaa kwa kiasi gani kwa wazazi kuwakusanya watoto wao pamoja nao kabla ya kula kifungua kinywa kuanza, kumshukuru Baba wa mbinguni kwa ulinzi Wake wakati wa usiku, na kumwomba msaada Wake na mwongozo na utunzaji Wake wakati wa mchana! Inafaa kwa kiasi gani pia, jioni ifikapo, kwa wazazi na watoto kukusanyika kwa mara nyingine mbele Zake na kumshukuru kwa baraka za siku ambayo imepita!

---

Watu walitawazwaje kuwa wafalme siku zile? Kwa nini watu walitaka mfalme? Kwa nini Samweli alisikitika? Kwa nini ngurumo ilikuja? Samweli alisema nini kingetokea asipowaombea Israeli? Ishara gani alipewa Sauli ya kuonesha yale aliyosema Samweli ni ya kweli?

**SIKU YA 76**
**(Machi 16)**

# Sauli Afanya Dhambi kwa Kufanya Huduma ya Kuhani

**– 1 Samweli 13-14**

Sauli alitawala Israeli miaka 40. Alichukua watu 3000 wa vita na kukaa nao. Alipokuwa ametawala kwa muda, Wafilisti walikuja kupigana na Israeli, naye akatuma ujumbe kwa Samweli aje ili atoe sadaka. Alingoja siku saba na Samweli hakuja, na hao watu walitawanyika mbali naye. Ndipo alipokosa uvumilivu na kufanya dhambi ya kuwaambia wamletee sadaka ya kuteketezwa na amani, na akaitoa kwa BWANA. Mara tu alipoitoa, Samweli akatokea, naye Sauli akaenda kumlaki na kumsalimu. Samweli akamwambia "umefanya nini?" naye akasema "Ni kwa sababu naliona ya kuwa watu wanatawanyika mbali nami, na wewe hukuja siku zile zilizonenwa na Wafilisti wamekusanyika pamoja kutujia."

Hata leo tunapaswa tuwe wavumilivu. Tukimwomba Mungu kitu na tunaona hajibu papo hapo, tuwe na imani kwamba atafanya kwa mema yetu. Mara zingine, haraka husababisha tufanye jambo baya ambalo ni vigumu kulisahihisha.

Sauli akasema aliogopa Wafilisti wakimshukia kabla hajaomba fadhili za BWANA na hivyo alijishurutisha kutoa sadaka ya kuteketezwa. Samweli akamwambia amefanya upumbavu kwa kutoshika Amri ya BWANA, Mungu, aliyomwamuru, "kwa maana BWANA angaliufanya ufalme wako kuwa imara juu ya Israeli milele. Lakini sasa ufalme wako hautadumu; BWANA amejitafutia mtu ampendezaye Moyo Wake, Naye BWANA amemwamuru yeye kuwa mkuu juu ya watu Wake, kwa sababu wewe hukulishika Neno lile BWANA alilokuamuru." Samweli aliondoka kwenda Gibea na Sauli akawahesabu watu aliokuwa nao 600 na akenda na mwanawe Yonathani. Hakuna aliyekuwa na zana yoyote au silaha isipokuwa Sauli na Yonathani. Naye Yonathani na kijana wake, wakaenda wawavukie Wafilisti bila ya kumwambia babaye. Akasema, "Na twende tukawavukie ngomeni hao wasiotahiriwa; yamkini BWANA atatutendea kazi; kwa maana hakuna la kumzuia BWANA asiokoe, kwamba ni kwa wengi au kwamba ni kwa wacache." Mchukua silaha alikubaliana naye akisema, "moyo wangu ni kama moyo wako". Wakaenda kuwavukia na kujidhihirisha kwao, wakasema wakiwaambia, ngojeni, hata sisi tuwafikilie; ila wakisema haya pandeni huku, tutajua kwamba Bwana amewatia mikononi mwetu, na hii ikawa ishara yao. Walipoenda na kujidhihirisha ngomeni mwa Wafilisti, Wafilisti walisema, "Waebrania wanatoka katika mashimo walimojificha," nao wakasema kwa Yonathani na mchukua silaha wake, wapande walipo nao watawaonesha jambo.

Basi walipanda kwa kupata hiyo ishara. BWANA alikuwa amewatia Wafilisti mikononi mwa Israeli. Wakawaua watu kama 20, kukawa na tetemeko kubwa katika

marago na katika shamba na katika watu wote, na watu wakatetemeka. Jeshi la Israeli likatawanyika, na Sauli akasema ni nani ametoka kati yao, na wakahesabu watu na kukuta hakuna aliyetoka isipokuwa Yonathani kijana wake na mchukua silaha wake. Sauli akaagiza Sanduku la Agano liletwe, ila kelele ilizidi kule kwa Wafilisti na akaacha mambo ya kumwambia kuhani alete Sanduku na akakusanya watu kwenda vitani. Kukawa na fujo kubwa, wakasikia Wafilisti wamekimbia na wakaanza kuwafuatia mbio vitani. Hivyo, "Bwana ndivyo alivyowaokoa Israeli siku ile. Waisraeli walisumbuka sana siku ile na Sauli aliwaapisha akisema asile mtu yeyote kitu cho chote hata jioni "nipate kujilipiza kisasi juu ya adui zangu." Watu walikubali na hawakuonja kitu, japo mwituni asali ilikuwapo ikidondoka na hakuna aliyetia mkono wake mdomoni wakiogopa kile kiapo. Ila Yonathani hakuwa amesikia kiapo cha baba yake na akanyosha ncha ya fimbo yake na kuchovya sega la asali, na kutia mkono kinywani na "macho yake yakatiwa nuru." Ndipo mtu mmoja aliyemwona akamwambia maagizo ya baba yake na kiapo alichoapa akisema, "alaaniwe mtu alaye chakula leo" na hata watu wamepungukiwa nguvu.

Ndipo Yonathani akasema, "Baba yangu amefadhaisha nchi" angalia jinsi nilivyopata nguvu na kuona vizuri baada ya njaa na kuchoka kwa sababu ya asali kidogo, watu wangekula na kushiba leo wangeteka nyara za adui zaidi. BWANA alikuwa amewapa ushindi, ila walishindwa kushambulia kwa nguvu kwa sababu ya njaa na uchovu. Watu walipoanza kula walikula kwa fujo, hata damu ya ng'ombe, ndipo Sauli alipowaambia "msikose juu ya BWANA, kwa kula na damu", basi walileta ngombe zao na kuchinja. Na kujenga madhabahu ya kumtolea BWANA sadaka. Walishuka na kuwafuata Wafilisti mpaka mapambazuko. Walipotaka kujua Neno la BWANA na wasipate jibu, waliamua kupiga kura kwamba ni kitu gani kimetokea. "Ikiwa dhambi i ndani yangu, au ndani yake Yonathani mwanangu Ee BWANA, Mungu wa Israeli, utuonyeshe." Basi kura ikamwangukia Yonathani kwamba ndiye mwenye kosa kwa kula asali. Sauli akamwambia "niambie ulilolifanya." Akamwambia kwamba alionja asali kidogo kwa ncha ya fimbo iliyokuwa mikononi mwake, na tazama imenipasa kufa. Sauli akasema hakika utakufa, ila watu wakamwambia Sauli, hatakufa Yonathani maana ndiye aliyeufanya huo wokovu mkuu katika Israeli. "Hasha! aishivyo BWANA, hautaanguka chini hata unywele mmoja wa kichwa chake; kwa maana ametenda kazi pamoja na Mungu leo." Hivyo watu wakamponya Yonathani asife. Hakika hatupaswi kufanya viapo visivyo na hekima. Sauli aliendelea kupigana na adui zake pande zote yaani, Moabu, Amoni, Edomu, Amaleki na Wafilisti, akitenda kwa ushujaa, na kuwapiga. Jemedari wa Jeshi la Sauli aliitwa Abneri, huyu alikuwa baba mdogo wa Sauli. Vita vikali vikaendelea siku zote za Sauli, naye Sauli alipomwona mtu yeyote hodari alimtwaa ili awe pamoja naye.

Yonathani anatufundisha kwamba ushindi hautegemei ukubwa wa Jeshi, silaha au utajiri. Bali tukiwa upande wa BWANA, sisi tu washindi. Akina baba wengi wasingependa kumuua mwana wao. Sauli lazima alijipenda mwenyewe na sifa yake mwenyewe kuliko mwana wake. Malaika wa mbinguni walimlinda Yonathani na mtumishi wake, nao wakapigana na Wafilisti mpaka wakaanguka mbele yao.
Daudi alikuwa nazo kasoro kubwa kama Sauli, ila tofauti kati ya wafalme hawa wawili wenye dhambi ni kuwa mmoja aling'ang'ania ufalme wake na mwingine alishikamana na Mfalme wa Wafalme. Na ni pale tu tunapokubali mapungufu yetu

na kuukubali utawala wa kweli wa Mungu kama Mfalme, ndipo tunapoweza kuwa 'mtu anayeupendeza moyo wa Mungu Mwenyewe.' Tusitoe visababu kama "Lazima nifanye kazi siku ya Sabato, kwa sababu mwajiri wangu alinilazimisha kufanya hivyo," au "Lazima nipokee hongo kwa sababu nahitaji pesa haraka," au "Lazima niseme uwongo, kwa sababu nililazimishwa," au "Sikurudisha zaka na sadaka kwa sababu bajeti yangu ilikuwa finyu sana," Visingizio vyote hivi havina uadilifu, na hatuna usalama isipokuwa tuwe na utiifu kamili kwa Neno la Mungu."

*Jitoe wakfu kwa MUNGU asubuhi; Valia njuga ili kuifanya hii kuwa kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako na liwe, "Nichukue, Ee Bwana, niwe wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni Pako. Nitumie leo katika huduma yako. Kaa nami, na kazi yangu yote ifanyike ndani Yako." Hili ni suala la kila siku. Kila asubuhi jitoe wakfu kwa MUNGU kwa ajili ya siku hiyo. Mkabidhi Yeye mipango yako yote, ili itekelezwe au ifanyike kulingana na jinsi Majaliwa Yake yatakavyoongoza. Kwa namna hiyo unakuwa unayatoa maisha yako mikononi mwa MUNGU siku kwa siku, na kwa njia hiyo maisha yako yatafanywa kuumbwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo.

Kwa nini Samweli alimwambia Sauli ufalme wake umepotea? Yonathani alisaidiaje kushinda vita Israeli? Kwa nini Sauli alitaka kumwua Yonathani? Ni nani alimwokoa Yonathani? Jemedari wa vita vya Israeli alikuwa nani? Kwanini ni dhambi kuacha kumwombea mtu mwenye dhambi?

**SIKU YA** 77
**(Machi 17)**

# Mungu Ajuta Juu ya Sauli Aliyejali Mapokeo Kuliko Utii

**- 1 Samweli 15-16**

Samweli alimwambia Sauli ujumbe kutoka kwa Bwana wa kuwapiga Waamaleki, kwa vile waliwatendea vibaya Waisraeli walipokuwa wakitoka Misri. Akatoa maagizo maalumu ya kuwapiga Waamaleki, na kuviharibu kabisa vitu vyote walivyo navyo. Sauli aliita watu na kuwahesabu watu 210,000 na kwenda vitani, akawapiga Waamaleki, akamkamata Agagi mfalme wao akiwa hai na kuwaangamiza watu wake kwa upanga. Sauli akamwacha Agagi hai, na kuchukua kondoo wazuri na ngombe na vinono, na kilicho chema, hakukubali kuviangamiza, ila kibaya na kibovu ndicho alichoangamiza kabisa. Neno la BWANA likamjia Samweli kusema, "najuta kwa sababu nimemtawaza Sauli awe mfalme; maana amerudi nyuma, asinifuate, wala hakufanya nilivyomwamuru. Samweli akasikitika, akamlilia BWANA usiku kucha. Akaondoka asubuhi na mapema amwone Sauli, naye alipomwona Samweli alisema, 'Ubarikiwe na BWANA, nimeitimiza amri ya BWANA." Hapa alikuwa anasema uongo, ndipo Samweli akasema mbona anasikia kilio cha kondoo na n'gombe masikioni mwake? Sauli akasema niliwaacha hai wanyama hawa ili kutoa dhabihu kwa BWANA, ila waliosalia wameangamizwa kabisa.

Basi Samweli akamwambia Sauli neno toka kwa BWANA akisema, "Ingawa ulikuwa mdogo machoni pako mwenyewe, Je! Hukufanywa kuwa kichwa cha kabila za Israeli? Naye BWANA akakutia mafuta uwe mfalme wa Israeli. Kisha BWANA akakutuma safarini, akasema, Enenda ukawaangamize kabisa wale Waamaleki wenye dhambi, upigane nao hata watakapoangamia. Mbona, basi, hukuitii sauti ya BWANA, bali ukazirukia nyara ukafanya yaliyo maovu machoni pa BWANA?" Sauli akabisha na kusema amewaangamiza, na hata akamleta Agagi mfalme wa Waamaleki. Ila nyara hizi za wanyama wazuri zimewekwa wakfu, kusudi vitolewe dhabihu kwa BWANA. Ndipo Samweli akamwambia kwamba BWANA hafurahishwi na dhabihu ila utii. Akamwambia, "angalia kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia kuliko mafuta ya beberu. Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi, na ukaidi ni kama ukafiri na vinyago; kwa kuwa umelikataa Neno la BWANA, Yeye Naye amekukataa wewe usiwe mfalme." Hapo ndipo Sauli alipoona kwamba Samweli anamaanisha kile anachokisema, na kwamba ndiye aliyemtawaza kuwa mfalme hapo awali. Hakujali sana kwamba hana utii kwa Mungu, bali nafasi yake ya ufalme. Ndipo Sauli akasema, "Nimefanya dhambi, maana nimehalifu Amri ya BWANA, pia maneno yako. Akasema kwamba aliwaogopa wale watu, akatii sauti yao. Sauli akasema, "Naomba unisamehe dhambi yangu, rudi pamoja nami nipate kumwabudu BWANA."

Samweli akakataa kurudi pamoja naye, kwa sababu amelikataa Neno la BWANA.

Naye Samweli alipogeuka, aende zake, Sauli alishika upindo wa vazi lake, nalo likararuka. Samweli akamwambia, “Leo BWANA amekurarulia ufalme wa Israeli, Naye amempa jirani yako, aliye mwema kuliko wewe. Tena, Yeye aliye nguvu za Israeli hatanena uongo, wala hataona majuto; maana siye mwanadamu hata ajute.” Naye Sauli akaomba msamaha, akiomba amheshimu sasa mbele za wazee na watu wake kwa kurudi na kumwabudu BWANA Mungu.

Samweli akakubali na kurudi nao wakamwabudu BWANA. Samweli akaamrisha aletewe Agagi, na Agagi akaenda akififikiri kuuawa kwakwe kumesahauliwa. Samweli akamwambia Agagi kwamba kwa sababu alikuwa amefanya wanawake wengi kuwa wajane, na watoto kuwa yatima, hivyo hata mama yake atafiwa. Samweli akamkata Agagi vipande huko Gilgali. Samweli akaenda kwake huko Rama na Sauli akaenda kwake huko Gibea, wala hakwenda tena kuonana na Sauli hata siku ya kufa kwake. Ila Samweli aliendelea kumlilia Sauli, Naye BWANA akaghairi kwamba amemtawaza Sauli awe mfalme juu ya Israeli. BWANA alimwambia Samweli, hata lini atamlilia Sauli, wakati Bwana amemkataa asiwalimiliki Israeli. Jambo la kusikitisha Muumba akihuzunika kwamba ametupatia mema. BWANA akamwambia nabii huyu aijaze pembe yake mafuta, na kwenda kwa Yese wa Bethlehemu, maana “nimejipatia mfalme katika wanawe.” Samweli akaogopa, ataendaje, maana Sauli akipata habari atamwua. Bwana akamwambia achukue ndama, na kusema ameenda kumtolea BWANA dhabihu. Naye amwite mzee Yese kwenye dhabihu. Naye alifanya vile, alipofika Bethlehemu wazee wa mji wakitetemeka wakasema “umekuja kwa amani mtu wa Mungu?” Naye akasema kwamba ameenda kutoa sadaka, na ni kwa amani. Akawaambia wajitakase na waje kwenye dhabihu. Alipowatakasa Yese na wanawe, akamwambia Yese awaite vijana wake; alikuwa na watoto wa kiume saba. Alimwita kijana wa kwanza Eliabu aliyekuwa mrefu na sura ya kupendeza, na Samweli akadhani huyu ndiye. BWANA akamwambia Samweli “Usimtazame uso wake, wala urefu wa kimo chake; kwa maana mimi nimemkataa. Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu hutazama sura ya nje, bali BWANA huutazama moyo.” Kisha Yese akampitisha kijana wa pili Abinadabu, mbele ya Samweli, akasema “BWANA hakumchagua huyu.” Yese akampitisha Shama, naye akarudia tena, “Bwana hakumchagua huyu”

Kutii ni bora kuliko dhabihu. Matendo mema hayawezi kamwe kuchukua nafasi ya utii.

Lakini wengi hufikiri Mungu anajali sana kuhusu zaka na sadaka zaidi ya utii. Siyo hivyo! Uasi hutuweka katika ushirika na shetani. Kufikiri na kutenda maoni yetu wenyewe ni kujiabudu wenyewe.

**Ombi: Bwana nisaidie kukupenda kwa undani zaidi; kukufuata kwa ukaribu zaidi, kunyenyekea Kwako kikamilifu zaidi, ili nipate kukusikia kwa uwazi zaidi. amina!**

*Lazima ujifunze kuona kwa akili yako na pia macho yako. Lazima uyaelimishe maamuzi yako ili yasiwe dhaifu, yasiyo na ufanisi au yasiyofaa. Ni lazima uombe kwa ajili ya uongozi, na kuweka njia yako kwa Bwana. Ni lazima uufunge moyo wako

dhidi ya upumbavu na dhambi zote, na kuufungua kwa kila mvuto au ushawishi wa mbinguni. Ni lazima utumie vizuri wakati na fursa zako, ili kusitawisha tabia yenye ulinganifu


---

Kwa nini Mungu alitaka Waamaleki waadhibiwe? Sauli alitoa udhuru gani wa kutoangamiza Waamaleki? Samweli alimwambia nini Sauli alipotoa udhuru? Baba ya Yese alikuwa nani? Kwa nini kuasi ni kama kuwa mchawi, na kuwa mkaidi ni kama kuwa kafiri? Je, Kuna ubaya gani kutazama sura ya nje tu ya mtu na siyo tabia?

**SURA YA 78**
**(Machi 18)**

# Daudi Achaguliwa Kuwa Mfalme

**- 1 Samweli 16-17**



Basi Yese aliwapitisha wanawe saba wote lakini Samweli akamwambia, “BWANA hakuwachangua hawa.” Kisha Samweli akamwuliza Yese kama watoto wake wote wamepita hapa. Yese akajibu, amebaki mdogo wao wa mwisho ambaye anachunga kondoo. Samweli akaamrisha mtu aende akamletee, kwa kuwa “hatutaketi hata atakapokuja huku.” Kweli lazima alikuwa kijana mwenye tabia nzuri na anayempenda Mungu, maana kama mtu wa Mungu mzee hataketi mpaka aje, lazima alikuwa na kitu huyu kijana mdogo wa Yese. Basi aliletwa Daudi, ambaye alikuwa mwekundu, na macho mazuri, na umbo lake lilikuwa la kupendeza. BWANA akamwambia, “ondoka, umtie mafuta, maana huyu ndiye.” Samweli akaitwaa pembe yenye mafuta na akamtia mafuta Daudi, na Roho ya BWANA ikamjia kwa nguvu tangu siku ile. Samweli akarudi zake Rama.

Daudi aliendа na kuwa mfalme mwenye nguvu, na mtu ambaye moyo wa Mungu ulielekea Kwake. Hata Masihi akaitwa kwa jina Lake, “Mwana wa Daudi.”

Roho wa BWANA alikuwa amemwacha Sauli, na roho mbaya ikamsumbua, hata watumishi wake wakaona roho mbaya au pepo wabaya wanamsumbua. Wakamwambia wamletee mtu stadi wa kupiga kinubi, ili pepo mbaya wa Shetani atakapomwingia, mpiga kinubi atapiga ili kumburudisha, naye atapona. Hata leo watu wengi wanateswa na pepo wabaya na sonona, na kinachowasaidia kupona ni Jina la Kristo. Basi Mtumishi mmoja akasema amemwona Daudi mwana wa Yese wa Bethlehemu, stadi wa kupiga kinubi, tena ni mtu shujaa na hodari wa vita, na anenaye kwa busara, mtu mzuri ambaye BWANA yu pamoja Naye. Daudi wakati huu alikuwa hajafikisha miaka 18, hivyo kwa umri wa kawaida tunasema alikuwa mtoto bado kwa miaka ya siku hizi. Watu walimjua Daudi, ushujaa wake, busara yake na hata uzuri wake. Kweli hata mtoto anajulikana kwa tabia yake. Basi Sauli alipeleka ujumbe kwa Yese kumwita Daudi, naye Yese akapeleka zawadi ya mikate, mbuzi na divai kwa mfalme na kijana wake. Mambo ya ajabu mfalme aliheshimiwa

sana, siku hizi ukiitwa ikulu kufanya kazi ya muziki, unalipwa, siku zile mfalme alipewa zawadi na watoto wake wakachukuliwa kama watumwa, kama BWANA alivyosema kupitia Nabii Samweli. Sauli akatuma ujumbe kwa Yese kwamba amwache Daudi akae kwake, maana alimpenda kwa tabia yake. Ikawa roho mbaya ilipomjia Sauli, Daudi alipiga kinubi kwa mkono wake na Sauli akaburudishwa na ile roho mbaya ikamwacha, kwani Roho wa Mungu alikuwa pamoja na Daudi. Watoto, siku hizi tunapoona watu wenye mapepo, tujue wanahitaji kuombewa kwa Mungu ili yawatoke. Watu wanaomkiri Mungu wa mbinguni na kuishi maisha ya utauwa wamesaidia wengi kutoa mapepo au majini, ambayo ni watumishi wa Shetani, au malaika walioasi. Hawa wanatesa watu mno, bali kwa Jina la Mungu au Kristo wanatoka.

Wakati huo Wafilisti walikusanyika kwa vita huko Yuda naye Sauli na Waisraeli wakakusanyika katika bonde kupanga vita juu yao. Wafilisti walisimama mlima wa upande mmoja na Waisraeli mlima mwingine, na katikati kulikuwa na bonde. Ndipo akatoka shujaa katika kambi ya Wafilisti, aitwaye Goliathi, mtu wa mji wa Gathi, ambaye urefu wake ulikuwa zaidi ya futi tisa. Huyu asingeweza kupita kwenye milango ya kawaida. Alikuwa na chapeo ya shaba kichwani, tena amevaa dirii ya shaba ya shekeli efu tano za shaba. Alivaa mabamba ya shaba miguuni mwake, naye alikuwa na mkuki wa shaba kati ya mabega yake; na mti wa fumo lake ulikuwa kama mti wa mfumaji na kichwa cha mkuki wake kilikuwa kama shekeli mia sita za chuma. Mtu aliyechukua ngao yake alimtangulia naye akasimama akipigia makelele majeshi ya Israeli na kuwakejeli, "Jichagulieni mtu, akanishukie mimi. Kama akiweza kupigana nami na kuniua, sisi tutakuwa watumwa wenu; nami nikimshinda yeye na kumwua, ninyi mtakuwa watumwa wetu, na kututumikia." Huyu Mfilisti akayatukana majeshi ya Israeli, basi Sauli na Israeli waliposikia maneno yake wakafadhaika na kuogopa sana. Daudi mwana wa Yese, alikuwa na kaka zake watatu wakubwa kwenye jeshi la Sauli. Daudi alikuwa akienda kwa Sauli na kurudi kulisha kondoo za babaye kule Bethlehemu. Goliathi alijitokeza asubuhi na jioni kwa siku 40 akiwatisha Waisraeli na kuwafadhaisha.

Siku moja Yese alimwambia kijana wake Daudi awapelekee bisi, jibini na mikate kaka zake watatu waliokuwa vitani, na awajulie hali yao na kuleta habari. Daudi aliondoka asubuhi na kuacha mifugo kwa mchungaji, akachukua chakula akaenda na kufika kwenye magari, wakati jeshi likitoka kwenda kupigana, na watu wakipiga kelele ya vita. Waisraeli walijipanga safu yao na Wafilisti safu yao wakikabiliana. Basi Daudi akaacha vyombo na chakula kwa mtu amlindie, kisha akalikimbilia jeshi kuwasalimu kaka zake Eliabu, Abinadabu na Shama. Alipokuwa akisalimia kaka zake, hapohapo yule shujaa Goliathi wa Gathi alitokea, na akasema maneno yale yale ya kuwakejeli na kuwatukana Waisraeli, naye Daudi akayasikia. Watu wote walipomwona walikimbia kwa woga mkubwa, wakisemezana kuhusu mtu huyu "hakika ametokea ili awatukane Israeli," wakasema kwamba yeyote atakayemwua, mfalme ametoa ahadi kwamba atampa mtu huyo utajiri mwingi na atamwoza binti yake na kuzawadia ukoo wake. Daudi akazungumza na watu kuhusu zawadi ya mtu atakayemshinda huyu Mfilisti. Alisema, "kwa maana mtu huyu kafiri asiyemjali Mungu ni nani hata awatukane majeshi ya Mungu aliye hai?" Watu wakamjibu zawadi ambazo mfalme ameahidi. Hapo kaka yake mkubwa

Eliabu alitokea na kumkuta akiongea na watu, na kwa hasira alimwambia mdogo wake kwa nini amekuja, na kuacha kuchunga kondoo. Aliona mdogo wake kwamba anataka tu kuja kutazama vita, au kutafuta umbeya. Eliabu akamng'akia mdogo wake, "Najua umeacha majukumu ili kuja kutazama vita tu." Daudi akasema "mimi nimekosa nini sasa?"

*Ombi kwa Ajili ya Mwongozo wa MUNGU linaweza Kutolewa Wakati Wowote, na mahali Popote—Hakuna wakati au mahali ambapo haifai kutoa ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu kwa roho ya maombi ya dhati. Katika umati wa watu mitaani, katikati ya shuguli au biashara, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kuomba mwongozo wa MUNGU, kama vile Nehemia alipotoa ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kuacha mlango wa moyo wazi daima na mwaliko wetu kwa Masihi ukiendelea kupanda juu ili Yesu aje na kukaa ndani yetu kama Mgeni wa mbinguni katika nafsi.

---

Daudi alikuwa na kaka wangapi? Majina yao ni yapi? Kwa nini Daudi hakupenda maneno ya Goliathi? Goliathi alivaa nini akienda vitani? Unawezaje kumsaidia mtu mwenye pepo wabaya au majini? Kwa nini watu hukazania kushugulikia uzuri wa nje zaidi, hata kuununua ikiwezekana?

**SIKU YA 79**
**(Machi 19)**

# Daudi na Goliathi, Vita ni vya Bwana na si Vyetu

**- 1 Samweli 17**



Daudi alishtuka kwamba hakuna mpiganaji stadi hata mmoja aliyediriki kulitetea Jina la Mungu baada ya siku 40 za matusi na kutamba kwa Goliathi. Hata Mfalme Sauli mtu mrefu kupita wote katika Israeli alikuwa amejikunyata. Daudi alikuwa na moyo wa kulitetea Jina la Yehova! Hakuzingatia ufupi au ujana wake, lakini alimwomba Mungu nguvu. Ikiwa tutazingatia mapungufu yetu hatuona kile Mungu anachokiona kwetu, yaani vyombo visivyokamilika ambavyo vinahitaji kujazwa na nguvu na uwezo Wake ili tuweze kumtukuza Mungu. Ibilisi anapotudhihaki kwamba Mungu hayupo na hawezi kuaminiwa, tunapaswa kukumbuka siku ambazo tumeshinda kwa msaada wa Mungu. Mungu anatuita kwenye mazingira yasiyowezekana ili atukuzwe kupitia udhaifu wetu. Daudi alitumia ustadi ambao tayari alikuwa ameufahamu, yaani kombeo. Alichukua hatua hiyo bila kujua matokeo yatakuwaje, lakini alitoka nje kwa imani. Mungu hahitaji ustadi wa kijeshi ili apate ushindi; Kile anachohitaji tu ni kujisalimisha kikamilifu. Kabla ya majeshi

ya adui kujisalimisha kwetu, ni lazima tujisalimishe kwa Mungu.

Mungu ametutajirisha kila mmoja wetu kwa vipaji vya kipekee kwa Utukufu wake. Usijali kwamba wewe si mzee, u mdogo, u dhaifu, au huna karama ya teknolojia. Njoo tu kwa Yesu jinsi ulivyo na umwombe akufanye ufanane Naye. Basi Yale maneno Daudi aliyosema yalimfikia mfalme Sauli, naye akatuma mtu kumwita Daudi. Daudi akamwambia Sauli kuwa mtu yeyote asizimie moyo kwa ajili ya Goliathi kwani yupo tayari kwenda kupigana na huyu Mfilisti. Sauli akamwambia Daudi "huwezi wewe kumwendea Mfilisti huyu upigane naye; maana wewe u kijana tu; na huyu ni mtu wa vita tangu ujana wake." Daudi akamwambia Sauli kwamba alipokuwa akichunga kondoo wa baba yake, simba au dubu walipotokea aliwafuata na kuwapiga, na kuwapokonya kinywani mwao kondoo za baba yake, na akimrukia, humshika ndevu zake, akampiga na kumwua. Akaeleza kwamba na huyu Mfilisti asiyemjali Mungu atakuwa kama mmoja wao, kwa sababu amewatukana majeshi ya Mungu Aliye hai. Daudi akasema, "BWANA aliyeniokoa na makucha ya simba, na makucha ya dubu, ataniokoa na mkono wa Mfilisti huyu." Sauli akamwambia Daudi, "Enenda, na BWANA atakuwa pamoja nawe." Ndipo Sauli akajaribu kumvika mavazi yake ya vita, Daudi alipojaribu kwenda, aliona ni vizito mno kwake, wala hakuweza kutembea vyema, basi akavivua, maana ilikuwa kama mtoto mdogo anayejaribisha nguo ya Baba. Daudi akachukua fimbo iliyo mkononi mwake, na akajichagulia mawe matano laini katika kijito cha maji, na kuyatia katika mkoba wake wa kichungaji aliokuwa nao.

Kisha akachukua kombeo lake mkononi na kumkaribia Goliathi. Mfilisti naye akamsogelea Daudi, na mtu wake aliyemchukulia silaha akamtangulia. Goliathi alipomwona Daudi alimdharau, kwa kuwa ni kijana tu mwekundu, mwenye sura nzuri, akamwambia Daudi, "Mimi ni mbwa hata, unanijia na fimbo?" Akamlaani Daudi kwa miungu yake, na kumwambia "njoo huku kwangu, nyama yako nitawapa ndege wa angani na wanyama wa mwituni." Hapo ndipo Daudi akamwambia Mfilisti maneno mazito yanayovuma mpaka leo, nawe wapaswa kuyakariri na kwa imani yabariki maisha yako. Maana ni ya kweli hata leo kwa maisha yako unapokabiliana na maadui. Alisema, "wewe unanijia mimi na upanga, na fumo na mkuki, bali mimi nakujia wewe kwa Jina la BWANA wa majeshi. Mungu wa majeshi ya Israeli uliwaowatukana. Siku hii ya leo BWANA atakuua mkononi mwangu, nami nitakupiga na kukuondolea kichwa chako, nami leo nitawapa ndege wa angani na wanyama wa nchi mizoga ya majeshi ya Wafilisti, ili kwamba dunia nzima wajue ya kuwa yuko Mungu katika Israeli. Na pia watu wote duniani wajue kwamba Bwana haokoi kwa upanga wala kwa mkuki; maana vita ni vya BWANA, naye atawatia ninyi mikononi mwetu."

Hapo ndipo Goliathi alipojiinua kwa kwenda kumkaribia Daudi kwa dharau. Daudi naye akapiga mbio akimfuata, nafikiri hili ndilo lilimchanganya kabisa, kwani majitu marefu kama Sauli yalikuwa yamemkimbia Goliathi, lakini huyu mtoto anamkimbilia uso kwa uso wakutane, akafikiri pengine mtoto huyu ana wazimu. Daudi alichukua jiwe moja na kuliweka kwenye kombeo yake, na kurusha jiwe lililompiga Goliathi kwenye kipaji cha uso, na akaanguka chini kifudi fudi. Jitu hili lilikuwa limejihami kila mahali. Pengine ilibakia sehemu ndogo sana iliyokuwa wazi, na hiyo ndiyo

Mungu aliitumia kumpatia Daudi ushindi. Watu hawakuamini, kwamba Daudi, kijana mdogo angeweza kumshinda mtu wa vita, bila hata upanga. Daudi akachukua upanga wa yule Mfilisti, na kusimama juu ya mwili wake, na akamwua kwa upanga huo. Wafilisti walipoona shujaa wao ameanguka, walikimbia. Waisraeli wakainuka na kupiga kelele, wakiwafuata hawa Wafilisti mpaka kwao Goliathi, kule Gathi, na miji mingine kama Ekroni. Waliteka nyara na kuwafukuza Wafilisti. Sauli akamwuliza Jemedari wake Abneri, "Je! Kijana huyu ni mwana wa nani?" Naye Abneri, hakujua, japo Daudi alikuwa amefanya kazi ya kumpigia mfalme kinubi ili kutoa pepo wachafu.

Hata leo Bwana anawapigania watu Wake. Inashangaza yale Mungu anayoweza kutenda kupitia kwa mtoto mdogo kama Daudi. Hata wewe leo, katika changamoto zako, hakuna ambacho Mungu anashindwa ikiwa tutamruhusu awe kiongozi wetu na tumtii. Kila tutakachoshika kukifanya kitafanikiwa endapo Yeye atakuwa namba moja katika maisha yetu. Daudi yaweza kuwa alisema Goliathi ni mkubwa sana huwezi ukakosa pa kupiga Bwana akiwa nawe.

Biblia inasema, "Kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho." Waefeso 6:12 . Wakati wowote watoto wa Mungu wanaposhambuliwa kwa ajili ya haki kuitetea haki, ni Shetani Ndiye anayewashambulia. Wanachohitaji kufanya ni kuhakikisha kwamba Mungu Yuko pamoja nao na kuamini kwamba Yeye Ndiye atakayewapigania kama alivyoahidi, na ushindi utakuwa wao (Kutoka 14:14). Lakini ni lazima watumie njia ya Mungu katika kupigana na adui zao. Njia Yake ni nini ? "Lakini Mimi nawaambia, wapendeni adui zenu, wabarikini wale wanaowalaani, watendeeni mema wale wanaowachukia ninyi, waombeeni wanaowadhulumu na kuwaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; kwani Yeye huliangazia jua Lake juu ya waovu na wema, na huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki." Mathayo 5:44-45.

*Ombi kwa Ajili ya Mwongozo wa MUNGU linaweza Kutolewa Wakati Wowote, na mahali Popote—Hakuna wakati au mahali ambapo haifai kutoa ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu kwa roho ya maombi ya dhati. Katika umati wa watu mitaani, katikati ya shuguli au biashara, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kuomba mwongozo wa MUNGU, kama vile Nehemia alipotoa ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kuacha mlango wa moyo wazi daima na mwaliko wetu kwa Masihi ukiendelea kupanda juu ili Yesu aje na kukaa ndani yetu kama Mgeni wa mbinguni katika nafsi.

---

Kwa nini Sauli alimpa Daudi mavazi yake ya vita? Kwa nini Goliathi alifikiri atashinda? Taja mambo matano yaliyomfanya Daudi ashinde. Kwa nini si vizuri kudharau watu japo wawe wadogo? Sauli alimwuliza nani kuhusu Daudi? Tunawezaje kumweka Mungu awe namba moja katika maisha yetu?

**SIKU YA 80**
**(Machi 20)**

# Urafiki wa Daudi na Yonathani

**- 1 Samweli 18-20**



Ikawa Daudi alipozungumza na Sauli, kijana wake Yonathani akampenda Daudi kama rafiki yake. "Roho ya Yonathani, ikaambatana na roho ya Daudi, Yonathani akampenda kama roho yake mwenyewe." Sauli akamtwaa Daudi siku ile, na hakumwacha arudi kwa baba yake tena, labda kusalimia tu. Yonathani akavua mavazi yake na kumpa Daudi, pia upanga, upinde na mshipi wake. Daudi akatoka kwenda kila alikotumwa na Sauli, akatenda kwa akili, Sauli akamweka awe juu ya watu wa vita, na jambo hili liliwafurahisha watu, hata wale waliomtumikia Sauli. Basi alipotoka kumwua Goliathi Mfilisti, wanawake walitoka na kuimba ili kumlaki mfalme Sauli kwa matari na shangwe na hata vinanda, wakiitikia pambizo "Sauli ameua elfu zake, Na Daudi makumi elfu yake." Wanawake hawa hawakufanya jambo jema kwani walishinda vita kwaajili ya Bwana na pia walikuwa ni wachochea ugomvi miongoni mwa wanaume wa nchi hiyo! Sauli aliposikia zile sifa alighadhabika, kwa sababu kama mfalme na mkuu wa nchi hakutaka mtu mwingine asifiwe kumzidi yeye, hivyo akachukia kwamba "wamempa Daudi makumi elfu, na yeye elfu tu."

Sauli aliona Daudi ni tishio kwa ufalme wake. Akaanza kumwonea kijicho Daudi toka siku ile. Ikawa roho mbaya ikamjia Sauli kwa nguvu, na Daudi alikuwa akimpigia kinubi kwa mkono wake kama siku zote, na Sauli aliyekuwa ameshika mkuki, akautupa kwa Daudi ampige ili amwue. Daudi akakwepa na akatoka mbele yake; jambo hili likatokea mara mbili. Sauli akamwogopa Daudi, akajua kuwa Bwana yu pamoja naye, na amemwacha yeye. Sauli akamweka Daudi awe kiongozi wa jeshi lake la askari elfu, Daudi alitenda kwa busara katika njia zake zote, Naye BWANA alikuwa pamoja naye, na Sauli akazidi kuogopa zaidi. Alikuwa mtu aliyemcha Mungu na kuwa na upendo wa kweli kwa watu, na unyenyekevu. Sauli akasema atampa Daudi binti yake wa kwanza, na akataka amweke katika mtego na Wafilisti; iwe si yeye atakayemwua bali Wafilisti. Daudi, akajibu kwa heshima, kwamba ni nani yeye katika Israeli hata awe mkwe wa mfalme. Lakini binti huyo wa kwanza akaolewa na mtu mwingine. Ndipo Sauli akampa Daudi

binti yake wa pili aitwaye Mikali, ambaye alimpenda Daudi sana. Sauli alikuwa na nia ya kufanya binti yake awe mtego au chambo cha kumwua Daudi. Daudi alisema yeye ni maskini na hana mahari kwa mfalme. Mfalme alikuwa ameahidi kwamba mtu atakayemwua Goliathi, atampa binti yake, lakini hakutunza ahadi yake. Sasa alibadili na kusema mtu atakayeua Wafilisti 100 atampa binti yake. Basi Daudi akafurahia jambo la kuwa mkwe wa mfalme, naye Sauli akamwoza bintiye Mikali, huyu akawa mke wa kwanza wa Daudi. Sauli akaendelea kutambua kweli kwamba Bwana yu pamoja na Daudi na akazidi kumwogopa, badala ya kufurahi kwamba mkwe wake ana sifa njema na sasa yeye ni mzee hivyo angepata mtu mwenye hekima wa kumrithi ufalme wake. Kila mara Daudi alitenda kwa busara zaidi ya watumishi wote wa Sauli, hivyo jina lake likawa na sifa kuu.

Wivu ni sumu mbaya kwani inapoteza muda wetu kwa mawazo machafu na kuharibu baraka zetu. Tukiona wivu kwa marafiki zetu tumuombe Mungu atoe chachu hiyo, na kumwomba Mungu kwa dhati awabariki wale tunaowaonea wivu. Mungu anawapenda watu wote. Anza leo kuondoa chuki nawe utaona furaha tele. Daudi alikuwa raia wa kawaida, ila mfalme mwenye cheo alimwonea wivu kwaajili ya kutawaliwa na mwovu.

Sauli alizungumza na wanawe ili wamwue Daudi. Yonathani mwana wa Sauli alimpenda Daudi, na akamwambia Daudi kila baba yake alipopanga dhidi yake. “Baba yangu, anatafuta kukuua; basi nakusihi ujiangalie sana asubuhi, ukae mahali pa siri na kujificha,” naye akasimama kando azungumze na babaye ajue kama anapanga kumwua ili amwambie Daudi. Basi Yonathani akamsifu Daudi mbele ya baba yake ili asikie atakachosema, na akamwambia baba yake asikose juu ya mtumishi wake Daudi, kwa maana yeye hajakosa kitu kwa kuwa “matendo yake ni mema siku zote.” Akamwambia jinsi alivyomwua Goliathi Mfilisti ili awaokoe. “Basi kwa nini kukosa juu ya damu isiyo na hatia, umwue Daudi bure?” Sauli ambaye alikuwa kigeugeu kwa vile Roho wa Mungu alikuwa amemtoka, aliapa akisema, “Kama aishivyo BWANA, yeye hatauawa.” Yonathani akamwambia Daudi, na kumleta mbele ya Sauli ili ahudhurie mbele zake. Kisha kukawa na vita na Daudi akatoka na kuua Wafilisti, na roho mbaya ikamjia Sauli na akatwaa mkuki tena na kumrushia Daudi wakati akimpigia kinubi mkononi mwake. Daudi akaponyoka mbele ya Sauli na akakimbia. Adui yako anaweza asiache kufuatilia kukuua, lakini Mungu hataacha kukulinda ikiwa saa yako ya kufa haijafika. hakuna awezaye kukunyakua mikononi mwa MUNGU.

Sauli akatuma wajumbe kumfuata mpaka nyumbani kwake, wamvizie na kumwua asubuhi. Naye Mikali mke wake akamwambia ajiponye nafsi yake maana baba yake anataka kumwua. Daudi akatelemshwa dirishani na mke wake na kutoroka, kisha Mikali akatwaa kinyago na kukifunika na nguo; na nywele akatia singa za mbuzi kichwani. Sauli alipotuma wajumbe kumleta Daudi kwenye kitanda chake, waliona kinyago na mto wa singa za mbuzi kichwani pake. Sauli akamgombeza binti yake, “mbona wewe umenidanganya hivi, na kumwacha adui yangu aende, hata ameniponyoka? Mikali akajitetea kwamba Daudi alitishia kumwua. Kweli ni uovu gani huu wa baba kumwambia binti yake amchague yeye na amwue mume wake? Cha kushangaza ni kwamba Sauli alimwagiwa Roho Mtakatifu akianza kazi,

ila aliamua kujifanyia anavyotaka. Basi Daudi alikimbia na kwenda Rama kwa Samweli, na kumwambia yote aliyotendewa. Wakaishi na Samweli kule, na ndipo Sauli alituma watu wakamkamate kule, na wale wajumbe walipofika kule na kuona jamaa ya manabii wakitabiri, nao walianza kutabiri, naye Sauli alipotuma wengine pia walitabiri. Sauli akatuma wajumbe mara ya tatu nao wakatabiri tena. Mwishowe alipoona wajumbe watatu hawarudi, alienda mwenyewe na alipofika kule akaanza kutabiri, naye akavua nguo zake, na kuendelea kutabiri mbele ya Samweli.

Daudi akatoka Rama akaenda kwa Yonathani na kumwambia, “Nimefanya nini? Uovu wangu ni nini? Dhambi yangu mbele ya baba yako ni nini, hata akaitaka roho yangu?” Yonathani alimtuliza kwamba hatakufa, kwamba baba yake humwambia mambo yote kabla hajafanya. Daudi akamwambia Yonathani, Sauli anajua kuwa wao wawili ni marafiki, na hivyo atakuficha analotaka kunifanyia, “iko hatua moja tu kati ya mimi na mauti.” Basi Yonathani akamwahidi Daudi kuwa atafanya vile atakavyo, na kama kawaida ya sikukuu ya mwandamo wa mwezi waliketi chakulani na kula pamoja, ila yeye Daudi alitaka ajifiche. Lakini alisema Sauli akiona hayupo atauliza kwako, nawe ujibu, “Daudi alitaka sana nimpe ruhusa, aende upesi Bethlehemu, mji wake akatoe dhabihu kwa jamaa yake ya mwaka.” Akisema vyema, ujue mambo si mabaya, ila akikasirika ujue ya kuwa amekusudia kunifanyia jambo baya. Akamwambia Yonathani akiona baba yake amekasirika, kwa ajili ya Agano la BWANA pamoja naye, amweleze kuliko amwache babaye amwue, ni heri yeye mwenyewe Yonathani amwue kama ana ubaya fulani. Yonathani akasema kama kuna uovu atamwambia. Basi walifanya Agano kati yao na BWANA Mungu wa Israeli. Hakika silaha yoyote itakayofanywa juu yako kukudhuru wewe haitafaa chochote kile. Mtu akikushtaki mahakamani, utamshinda. Hilo ndilo fungu nililowapangia watumishi wangu. Hizo ndizo haki nilizowathibitishia. Mimi Mwenyezi-Mungu nimesema (Isaya 54:17). Roho Mtakatifu anapomwacha mtu, pepo mchafu anachukua nafasi yake na roho mbaya itamfanya mtu huyo kufanya mambo ya kutisha. Hebu tuepuke Roho Mtakatifu kutuacha. Kuendelea katika dhambi bila kutubu humfukuza Roho Mtakatifu (Waefeso 4:30). Wivu na kijicho ni magonjwa ambayo huvuruga uwezo wote wa kiumbe cha Mungu, na tabia hizo zilitoka kwa Shetani. Watu wengi huwa na tamaa ya kutawala, au mali kwa njia mbalimbali. Karibu napoishi kuna mtu alisema anauza viwanja mwezini juu, yaani km 382,500 kutoka duniani, kwa dola sita kwa ekari. Alipata watu milioni sita waliolipa ili kuweza kupata ardhi na kuweza kuishi huko! Hivyo alikuwa na dola milioni sita za kutapeli watu. Kwani hakuwa hata na ndege. Binadamu anatafuta mahali pazuri kiasi kwamba ni rahisi kudanganywa na mtu yoyote mwenye tamaa. Wengine wangependa sana kuishi anga za juu, na ndiyo maana Elon Musk ambaye anaunda magari ya umeme ya Tesla ametoa ofa ya watu wanaotaka kuchukuliwa huko kwenye anga la km 400 tu na roketi kwa dola 55 milioni tu! Hakika hatuna haja ya kuishi kwenye ndoto za Abunuwasi au maisha ya kufikirika. Tuna ushuhuda wa kutosha wa kile ambacho Mungu ameahidi tukiwa Waaminifu katika kufuata maagizo Yake, Yeye Mwenyewe atatutembeza mbali na mwezini hapa tunapopaona kwa macho yetu. Tutaenda kuvinjari mara kwa mara mbinguni na sayari zingine ambapo watu hawajaweza kufika bado. Ahadi ya ajabu iliyoje hii! (Angalia google)

Tukirudi kwa marafiki wawili, tunaona urafiki wa uaminifu wa ajabu wa vijana hawa wawili ulikuwa na nguvu, na hata walikuwa tayari kufa. Yonathani alikuwa tayari kuacha ufalme pia. Mfano huu ni kama wa Yohana mbatizaji, huyo alikuwa tayari Kristo ainuliwe juu mbele, naye ashuke. Urafiki wa wale wampendao Mungu unajenga tabia. Hebu tumtazame Kristo kama Yonathani, hakika tutakuwa wapole na wanyenyekevu na kujifunza tabia Yake bora! Mbingu humwona yule anayebeba amani na upendo kama balozi wa mbingu. Mtu kama huyo atapata thawabu yake. Atasimama katika siku kuu ya Bwana kama mshindi.

*Malaika Wako Karibu sana Kusaidia Tunapoomba Mwongozo wa MUNGU—Kama Nathanaeli, tunahitaji kujifunza Neno la MUNGU kwaajili yetu wenyewe, na kusali kwa ajili ya kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Yeye aliyemwona Nathanaeli chini ya mtini atatuona sisi mahali pa sirini pa maombi. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru wako karibu na wale ambao kwa unyenyekevu wanatafuta mwongozo wa Bwana.

---

Kwa nini Yonathani alimpa Daudi mavazi yake? Wanawake waliimba maneno gani ambayo yalimkasirisha mfalme Sauli? Je, unawezaje kuepuka kuchonganisha watu? Sauli alimwambia Daudi atoe mahari gani ili kuoa binti yake? Mke wa kwanza wa Daudi aliitwa nani? Mikali alifanyaje ili Daudi atoroke mauti? Kwa nini Sauli alimwogopa Daudi? Daudi alitoa udhuru gani kutokuwa kwenye sikukuu ya mwandamo wa mwezi?

**SIKU YA 81**
**(Machi 21)**

# Sauli Aua Makuhani, Baada ya Daudi kuzungumza nao

**- 1 Samweli 20-22**

Yonathani aliahidi kutomficha Daudi kama kuna neno litakalomfaa au la usalama kwake. Akaongeza "BWANA anitende mimi, Yonathani, hivyo na kuzidi ikiwa yampendeza baba yangu kukutenda mabaya, nisipokufunulia haya, na kukupeleka uende zako kwa amani, na Bwana awe pamoja nawe, kama alivyokuwa pamoja na baba yangu." Yonathani akijua kuwa Mungu amempa Daudi ufalme, alimkumbusha kutenda fadhili kwake na uzao wake "wakati ule BWANA atakapokuwa amewaondoa kabisa adui za Daudi wote pia katika uso wa nchi."

Yonathani akamwapisha mara ya pili Daudi kwa ajili ya upendo alikuwa nao kwake, maana alimpenda kama alivyoipenda roho yake mwenyewe. Akamwambia kwamba kesho yake siku ya mwandamo wa mwezi ashuke, naye atapiga mishale mitatu kama analenga kupiga shabaha, kisha atatuma mtoto kuifuatia ile mishale. Akimwambia mtoto mishale iko upande wako huu, "itwae uje, basi kuna amani, bali akisema mishale iko huko mbele zako", aondoke maana kuna hatari. "BWANA Yu kati ya wewe na mimi milele" kwa habari ya neno lile tulilolinena.

Daudi alijificha na asiende chakulani. Yonathani na Abneri walikuwa katika viti vyao na wahusika wote isipokuwa Daudi. Sauli hakusema neno, akifikiri Daudi ana dharura fulani, lakini siku ya pili, alipomkosa Daudi kwenye kiti chake alimwuliza Yonathani, akijua ndiye rafiki yake. "Mbona mwana wa Yese haji kula chakula jana wala leo?" Yonathani akajibu kwamba Daudi alimwomba ruhusa ya kwenda kwao kutoa dhabihu. Basi hasira ya Sauli ikawaka kwa mwanawe Yonathani, akasema, "Wewe mwana wa mke mkaidi, asi, je! Mimi sijui ya kuwa umemchangua huyo mwana wa Yese, kwa aibu yako mwenyewe…" Akamwambia Daudi akiwa kwenye ufalme, yeye hatafanikiwa kitu, wala hatapata ufalme. Akamshurutisha Yonathani amlete Daudi, ili afe. Yonathani akajibu, kwa nini auwawe, "Amefanya nini?" Sauli akamtupia mkuki kwa hasira kali, wala hakula chakula, kwa sababu alimhuzunikia Daudi sana, na kwa sababu baba yake amemwaibisha. Sauli alichaguliwa toka katika hali ya raia wa kawaida, wala baba yake hakuwa mfalme, ila sasa alikuwa na kiburi akitaka ufalme wake udumu. Hata leo, cheo na madaraka yanalewesha wengi, kabla ya kuyapata watu wanakuwa wanyenyekevu, lakini wakiyapata wananyanyasa wanadamu wenzao na kuua wengine. Wengine katika madaraka wanapenda watu wawaabudu, na kuwapigia magoti. Hata wewe mtoto, siku za usoni, Bwana akiwa bado hajarudi, unaweza kuwa na madaraka, kwa watoto wako, kwa mke wako au familia yako, kwenye shule yako, au hata serikalini. Je! Utayatumiaje madaraka hayo? Mwombe Mungu akupatie unyenyekevu ili usiwatese wajoli wako.

Asubuhi Yonathani alitoka kama alivyoagana na Daudi kwa ile ishara ya mishale, ila yule mtoto aliyemtuma hakujua, na Daudi akapata ujumbe. Kisha Yonathani alimpa mtoto silaha zake azipeleke mahali pake. Daudi alitoka alipojificha na kuanguka kifudifudi mara tatu, nao wakabusiana, na kulia pamoja. Yonathani akamwambia Daudi, “Enenda kwa amani; kwa maana sisi sote wawili tumeapiana kwa jina la BWANA kwamba, BWANA atakuwa kati ya mimi na wewe na kati ya uzao wangu na uzao wako milele.” Waliagana, na ndiyo ilikuwa mara ya mwisho kuonana wakiwa ikulu. Daudi akimtegemea Mungu alikuwa na amani katika dhiki kubwa iliyompata miaka mingi. Aliendelea kumsifu BWANA kwa zaburi akijua Mungu ni Baba yake, na hivyo atamlinda. Hebu nasi leo tupate faraja hiyo kwa kuwa Mungu ni baba yetu.

Daudi akaenda Nobu kwa kuhani mkuu Ahimeleki. Kuhani mkuu akamlaki akitetemeka, kwamba kwa nini yupo peke yake pengine alitegemea awe na watu wanaomsindikiza au na mfalme mwenyewe. Daudi akasema uongo kwamba ametumwa na mfalme, na akaomba mikate mitano. Aliambiwa hakuna mikate ila ile ya wonyesho inayokaa hekaluni na kubadilishwa kila wiki. Akaulizwa kama amejitakasa ili aweze kupewa, naye akasema ndiyo. Siku hiyo palikuwa na mpelelezi wa mfalme aliyeitwa Doegi Mwedomi, naye alienda kupeleka habari hizi kwa mfalme. Daudi akaomba kutoka kwa kuhani upanga au mkuki. Naye kuhani alisema upanga uliopo ni ule wa Goliathi wa makumbusho. Kuhani akamwambia akipenda kuuchukua auchukue. Basi Daudi aliuchukua, na kukimbia toka siku ile kwa hofu ya Sauli kutaka kumwua, akaenda kwa Akishi mfalme wa Gathi, Mfilisti. Na watu wa Gathi wakamwuliza Akishi, “Huyu siye yule Daudi, mfalme wa nchi?” Watu waliimba sifa zake, Sauli ameua elfu, naye ameua maelfu kumi.

Daudi aliposikia haya, akamwogopa Akishi, na kubadilisha mwendo wake akijifanya ana wazimu, akajikuna kuna kwenye mbao za mlango na kuacha mate yaanguke kwenye ndevu zake. Kisha Akishi akawaambia watu wake, kwa nini wamletee mtu mwenye wazimu? “Je, mimi nina haja ya watu wenye wazimu, hata mmemleta kiumbe hiki ili aonyeshe wazimu wake machoni pangu? Je! Huyu ataingia nyumbani mwangu?”

Daudi akatoka huko na kukimbilia pango la Adulamu na ndugu wa ukoo wake wakamwendea huko. Kila aliyekuwa na dhiki, uchungu au deni wakakusanyika kwake, naye akawa jemadari wao, wakapata watu 400. Daudi akaenda Mispa kule Moabu na kuzungumza na mfalme ili wazazi wake wakae huko, akisema, “hata nitakapojua Mungu atakalotenda kwa ajili yangu.” Hii inaonesha kwamba aliwapenda wazazi na kuwasaidia. Moabu ilikuwa kule bibi yake mzaa Baba, Ruthu alipotoka. Daudi anatoa mfano mzuri hapa wa kuwatunza wazazi wake uzeeni, kwa kutoacha Sauli awadhuru. Nabii wa Mungu Gadi alimwambia Daudi aende nchi ya Yuda, akakaa msitu wa Herethi. Sauli alisikia kuwa Daudi ameonekana alipokuwa Gibea. Sauli alikuwa na mkuki mkononi mwake, na watumishi wake wakamzunguka, naye akawaambia wa kabila lake kwamba Daudi hawezi kuwasaidia ila atawafaya wao kuwa maakida tu, hivyo wasifanye fitina naye, wamwambie siri zote za Daudi “hapana mmoja wenu anayenisikitikia, wala kunifunulia ya kuwa mwanangu

amemwondokesha mtumishi wangu juu yangu anivizie kama hivi leo." Daudi hakuwa anamvizia Sauli, bali kinyume chake, ila alitaka watu wamchukie Daudi na kisha wamwonee huruma yeye.




Doegi Mwedomi aliyeona Daudi akichukua panga kwa kuhani alienda kwa Sauli na kusema yote aliyoyaona Nobu kwa Ahimeleki. Alipoeleza kisa chote, ndipo mfalme Sauli alituma habari kumwita Ahimeleki kuhani, na makuhani waliokuwa Nobu, nao wakaenda kwa mfalme wote. Sauli akasema wamefanya fitina juu yake, kwa kumpenda Daudi kwani, wamempa mikate na upanga ili amvizie. Ahimeleki alijibu kwa heshima, kwamba "katika watumishi wako wote ni nani aliye mwaminifu kama Daudi, aliye mkwewe mfalme, tena msiri wako, mwenye heshima nyumbani mwako." Kuhani akasema si mara moja tu amemwuliza Mungu kuhusu Daudi, "hasha mfalme asinidhanie, mimi mtumishi wake neno hili." Akaongeza kwamba yeye hajui hayo yote, yaliyopungua au yaliyozidi, bali alifanya kwa nia njema tu. Mfalme alimwua kuhani na jamaa za baba yake katika ule mji wa kuhani, "hao makuhani wa Bwana … kwa sababu mkono wao u pamoja na Daudi." Akasema walijua Daudi amekimbia wasiniarifu. Watumishi wa mfalme walikataa kuangukia makuhani, bali Doegi akawaua makuhani 85 siku hiyo, na kuupiga Nobu, mji wa makuhani kwa upanga, yaani wanaume, wanawake, watoto, wanyonyao, na mifugo. Akaokoka mwana mmoja tu wa kuhani aitwaye Abiathari.

Daudi hakuwa mkamilifu, ingawa alikuwa mtu aliyeupendeza moyo wa Mungu mwenyewe. Yesu Peke Yake Ndiye alikuwa mkamilifu. Kwa hiyo, Yesu Ndiye mfano wetu, na siyo Daudi. Daudi aliwalaani adui zake ( Zaburi 35), lakini Yesu aliwaombea Adui zake (Luka 23:34). Daudi alikuwa na wake kadhaa na masuria (2 Samweli 16:21,22), Yesu anatufundisha kuwa na mke mmoja (Mt.19:4-6). Kati ya watu wote ambao wamewahi kuishi katika ulimwengu huu, ni Yesu pekee Yake ambaye hakuwa na dhambi. Yeye Ndiye kiwango au kipimo chetu. Hakuna mwenye haki wala hata mmoja. Kwa hiyo wale wote wanaomnukuu Daudi ili kuhalalisha kuwalaani adui zao au kuoa wake wengi wanafanya kosa kubwa, kwa sababu Mungu hajamweka Daudi kama mfano wetu wa kufuata, Yesu Ndiye ambaye Mungu ametupa kuwa Mfano wetu. Hebu mfuate Yesu, kwa maana Yeye Ndiye njia, na Kweli, na uzima, mtu haji kwa Baba ila kupitia Kwake Yeye. Mfano wa watu wema katika historia takatifu, ni wa kuigwa nasi pale tu, walipofuata nyayo za Bwana.

*Ujuzi wa Ukweli hautegemei sana nguvu ya akili kama ilivyo juu ya usafi wa kusudi la moyo, usahili wa imani ya dhati inayomtegemea Mungu. Kwa wale ambao kwa unyenyekevu wa moyo, wanaotafuta mwongozo wa MUNGU, malaika wa MUNGU huwakaribia (karibu). Roho Mtakatifu ametolewa ili kuwafungulia hazina nyingi za ile Kweli.

---

Yonathani alimwapisha nini Daudi? Sauli alimkaripia Yonathani kwa maneno gani? Kwa nini Sauli aliua makuhani 85 wa Bwana? Kwa nini alichofanya Doegi kilikuwa ni uovu? Kwa nini Daudi aliwatafutia wazazi wake mahali pa kuishi? Kwa nini Ahimeleki aliogopa alipomwona Daudi? Kwa nini watu hujisahau wapatapo cheo? Kwanini Yonathani alikuwa tayari kuhatarisha maisha yake?

**SIKU YA 82**
**(Machi 22)**

# Abiathari Akimbilia kwa Daudi

**- 1 Samweli 22-24**

Abiathari alipoona ndugu zake na familia yake imeuawa alikimbilia kwa Daudi, na kumweleza yaliyotokea, na Daudi akakumbuka Doegi Mwedomi alikuwa pale siku ile alipoenda kuomba chakula na upanga. Akasikitika masikitiko makuu kwa kuleteleza vifo vya jamaa za baba yake. Daudi akamwambia "kaa wewe pamoja nami, usiogope; kwa maana yeye atafutaye roho yangu, ndiye atafutaye na roho yako; nawe utakaa kwangu salama." Alimtia moyo. Wakasikia habari kuwa Wafilisti wanapigana vita Keila na kuiba nafaka shambani, Daudi akamwuliza BWANA kuwa aende, Naye BWANA akamwambia aende aiokoe Keila. Watu wake walikuwa na woga lakini Daudi akamwuliza BWANA Naye akajibu "Nitawatia hao Wafilisti mikononi mwako." Wakaenda, na kwa mashambulizi makali waliteka nyara, na kuiokoa Keila. Abiathari alienda na nguo za kikuhani kule. Sauli akasikia Daudi yupo Keila, akafikiri Mungu amemtia mikononi mwake na kushuka kule; Daudi akajua Sauli amekusudia mabaya. Daudi akamwuliza kuhani Abiathari aliyekuwa na naivera kujua kwa BWANA kama watu wa Keila watamuuza kwa Sauli; BWANA akamwakikishia kuwa ashuke tu na atakuwa pamoja naye. Akaenda na watu 600 kule, na Daudi aliendelea kukaa nyikani, ngomeni na milimani akimkimbia mfalme katili, Sauli. Sauli alikuwa akimtafuta kila siku, ila Mungu hakumtia mikononi mwake. Daudi akakaa katika nyika za Zifu, na Yonathani alimfuata kule na kumwambia "usiogope" maana mkono wa baba yangu Sauli hautakupata, nawe utakuwa mfalme wa Israeli, nami nitakuwa makamu wako, hata baba yangu anajua. Wakafanya tena Agano mbele za Bwana, na Yonathani akaenda nyumbani kwake. Urafiki huu unatuonesha uaminifu wa ajabu, kwamba unampenda mtu na kumtetea kwa vile ni mwema, na kutokuwa na ukabila au upendeleo wa kumchagua mwovu, eti kwa vile ni ndugu yako.

Watu wa Zifu walikwea wajipendekeze kwa Sauli huko Gibea, ili wamwuze Daudi, wakisema amejificha ngomeni mwao. "Basi sasa, Ee mfalme, ushuke, kama utakavyo…na kazi yetu itakuwa kumtia mikononi mwa mfalme." Sauli akawabariki watu wa Zifu kwa kumhurumia na kuwatuma wapate hakika zaidi pale alipojificha, maana ana "hila nyingi." Wakaondoka, kupeleleza wakati Daudi yuko nyika ya Araba, wakamwambia Daudi ashuke. Wakaanza kutafutana kwenye mlima, Daudi alienda kujificha kwa hofu ya Sauli maana hakutaka kumwua mpakwa mafuta wa BWANA. Sauli akiwa anamzunguka Daudi na jeshi lake, alisikia kuwa Wafilisti wameishambulia nchi yake, na hivyo Sauli akaahirisha uovu wake akarudi! Ndipo Daudi akaenda kwenye ngome huko Engedi. Sauli aliporudi kuwafuatia Wafilitsti, akaenda kumtafuta Daudi huko Engedi na watu elfu. Akafika kwenye pango ambalo Daudi alikaa na watu wake kwa ndani. Watu wakamwambia Daudi kwamba imefika siku ya BWANA kumtia adui yako mikononi mwako nawe utamtenda yoyote utakayoona mema. Basi Daudi alienda na kuukata upindo wa vazi

lake Sauli, na akakataa kabisa kumdhuru. Alisema, "Hasha! nisimtendee bwana wangu, masihi wa BWANA neno hili, kuunyosha mkono wangu juu yake, kwa maana yeye ni masihi wa BWANA." Daudi akazuia jeshi lake kwa maneno haya, akawakanya wasimshambulie Sauli. Sauli alitoka kwenye pango akaenda zake, na Daudi akatoka pangoni amwite Sauli na kumwonyesha kipande cha nguo yake. Mfalme alipomtazama Daudi na kwamba amemwacha bila kumdhuru, alisujudu hata nchi. Daudi akamwambia Sauli kwa nini ameyasikiliza maneno ya watu kwamba "Daudi anataka kukudhuru?" Akamwambia, leo hivi ameona jinsi BWANA alivyomtia mikononi mwake pangoni, na watu wake awaue, ila aliwaacha, akisema hataki kunyosha mkono wake kwa mpakwa mafuta wa BWANA.

Akamwambia aangalie upindo wa vazi lake, na kwamba aliukata bila kumwuua, basi ajue yeye hana uovu wala kosa mkononi mwake kama vile watu walinena, ingawa yeye Sauli alikuwa anamwinda roho yake. Daudi akasema, "BWANA anilipize kisasi changu kwako, lakini mkono wangu hautakuwa juu yako." Sauli alikuwa anamwinda na kumfuatilia japo yeye hakuwa na madhara kwake. Anajisumbua ili kumdhuru mtu asiye na hila kwake. "BWANA atuamue, akatuhukumu mimi na wewe, ukaone, akanitetee neno langu, akaniokoe na mkono wako" Daudi alimalizia.

Daudi alipomwambia Sauli hayo, Sauli akasema kwa huzuni "hii ndiyo sauti yako Daudi mwanangu?" naye akapaza sauti yake, dhamira ikimshtaki akalia kwa uchungu, "wewe u mwenye haki kuliko mimi, maana wewe umenitendea mema, nami nimekutendea mabaya. Nawe umeonyesha leo jinsi ulivyonitendea mema." Sauli akambariki akisema. "BWANA akulipe mema kwa haya uliyonitendea leo." Akambariki akisema anajua BWANA amempa ufalme, na ufalme utakuwa imara akiwa mfalme "basi uniapie kwa BWANA, ya kwamba hutawaua" ukoo wa baba yangu, na kuliharibu jina langu. Daudi alimwapia, kisha Sauli akaenda na watu wake, na Daudi akaenda ngomeni.

Kusamehe na kutolipa kisasi ni karama muhimu. Watu kama Sauli wenye chuki na wivu, hata wakisamehewa hawatambui. Tukumbuke, Mungu hawezi kuwasamehe wale wasiosamehe. Maana hakuna binadamu asiyekosea wengine au kukosewa! Mtu anapokataa kuwajibika kwa makosa yake ni vigumu kusamehewa. Sauli alijua hakufuata amri ya Bwana na badala ya kutubu kwa unyenyekevu kwa kumtendea Mungu dhambi, alihuzunika kuwa atapoteza nafasi yake kama mfalme. Sauli alipatwa na ugonjwa wa Lusifa, na kugeuka kuwa mbishi na kugeuza kibao, akisema Daudi alikuwa akijaribu kumuua wakati kiukweli yeye ndiye alitaka kumuua. Ikiwa tunakataa kutubu kwa dhati kwa ajili ya makosa yetu, na tunajaribu kuwabandikia dhihaka na hatia watu wa Mungu, badala ya kuwajibika na dhambi hiyo, basi kuna shida maana 1 Yohana 1:9 iko wazi "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

*Chochote Tunachohitaji, Tunaweza Kudai Katika Ombi—Kila ahadi katika Neno la MUNGU hutupatia mada kwa ajili ya ombi (kila ahadi hutupa jambo la kuombea, zipo ahadi zaidi ya 6000 kwenye Biblia!), ikiwasilisha Neno la Yehova lililoahidiwa kuwa uhakikisho wetu. Haijalishi baraka yoyote ya kiroho tunayoiihitaji, sisi

tumependelewa kuiomba kupitia Yesu. Tunaweza kumwambia Bwana, kwa usahili na unyenyekevu wa mtoto, kile tunachohitaji haswa. Tunaweza kumwambia mambo yetu ya muda mfupi yanayopita, tukimwomba mkate na mavazi na Mkate wa Uzima na joho la haki ya Kristo. Baba yako wa mbinguni anajua kuwa unahitaji vitu hivi vyote, na umealikwa kumwomba juu ya vyote. Ni kupitia Jina la Yesu kwamba kila neema inapokelewa. MUNGU ataheshimu Jina hilo, na atakidhi mahitaji yako kutoka katika utajiri wa ukarimu Wake.

---

Yonathani alikuja kwa Daudi kufanya nini? Kwa nini Sauli alikuwa na maneno ya toba kwa Daudi bali hakuacha uovu? Kwa nini Sauli alimbariki Daudi? Kwa nini Daudi hakumwuua Sauli? Je, watu walimwambia kweli Sauli kwamba Daudi ni adui yake? Inakuwaje Sauli alipenda kufanya uovu japo alikuwa anajutia? Baadhi ya watu hupenda kufanya mambo mabaya na kusema hakuna ubaya kutenda hivyo kwa sababu Daudi alifanya vivyo hivyo, watu kama hawa utawaambiaje?

**SIKU YA 83**
**(Machi 23)**

# Daudi, Nabali na Abigaili

**- 1 Samweli 25**



Samweli akafa na Israeli ikamwomboleza, na kumzika kwake Rama. Daudi akaenda Maoni nyikani, na jeshi lake pamoja na familia zao. Huko Maoni alikuwako mtu aitwaye Nabali. Mtu huyu alikuwa na mali nyingi, kama kondoo 3000, na mbuzi 1000. Huyu alikuwa akikata manyoya ya kondoo zake. Mke wake aliitwa Abigaili, naye alikuwa na akili njema, hekima, na uzuri wa uso. Basi Daudi akiwa nyikani na jeshi waliishiwa chakula, naye akatuma vijana kumi, kwa Nabali waende kumsalimia na kumwomba chakula, wakisema "wachungaji wako wamekuwa pamoja nasi, wala hatukuwadhuru, wala hawakukosa kitu wakati wote walipokuwako nasi huko Karmeli. Waulize vijana wako nao watakuambia." Akamsihi awape "chochote watumwa wako na mwanao Daudi." Walipofika na kumwambia Nabali, aliwajibu kwa ukali, "Daudi ni nani? Au mwana wa Yese; siku hizi watumwa wengi wanawatoroka bwana zao, kwa nini nitwae mkate wangu na maji yangu na machinjo yangu ... na kuwapa watu ambao sijui wametoka wapi." Watumishi walirudi kwa Daudi na kumwambia majibu ya Nabali, naye Daudi kwa hasira, akaliambia jeshi lake la watu 400 wajifunge na panga zao, na watu 200

wakalinda vyombo vyao. Ni jambo la hekima kutotenda kwa pupa na haraka kwa sababu mtu fulani amekudharau kwa namna fulani. Ni vizuri kutafakari, kutathmini upya na kucheua jambo hilo kwa makini. Hata kama Daudi alikuwa raia mwema wakusaidia watu, hakupaswa kulazimisha fadhila, au kufanyiwa karamu. Daudi alishukuru kwa hekima ya Abigaili kwasababu ilimfanya afikirie upya na afanye vile Ambavyo vingempendeza Mungu.

Bahati nzuri kijana mmoja alimpasha Abigaili yale mume wake aliyosema, na vile Daudi alivyonuia kudhuru watu wa mji huo. Kijana akamwambia Abigaili kwamba Daudi alituma watu kuwasalimu, naye bwana wao Nabali aliwatukana, ila watu hawa wa Daudi waliwatendea mema, na kuwasaidia kulinda mifugo yao isipotee walipofuatana nao, "watu hao walikuwa boma kwetu usiku na mchana… tukiwachunga kondoo." Akamsisitizia Abigaili, ajue na kufikiri atakayotenda, maana Daudi amekusudia mabaya kwa Nabali na mji wote. Maana Nabali ni mtu asiyefaa kabisa, na hivyo hawezi kumsikiliza mtu akizungumza naye. Ndipo Abigaili akafanya haraka na kutwaa mikate 200, viriba vya divai, kondoo watano walioandaliwa tayari kwa kula, bisi, vishada mia vya zabibu na mikate ya tini mia mbili. Akapakia vitu hivi juu ya punda na akafuatana navyo mwenyewe, na kuwaambia vijana wake watangulie mbele yake naye atawafuata, ila hakumwambia mume wake. Mwanamke huyu ni mfano mzuri wa hekima wa jinsi ya kuishi na "watu wasiofaa" hasa katika ulimwengu wa leo. Akatelemka na punda, akamwona Daudi na watu wake wakishuka kumkabili, na Daudi alikuwa ameshasema kwamba amefanya kazi bure na watu wake kuwalinda watumishi wa Nabali wasipotewe na mali, nao sasa wana njaa na hawana chakula, na "amewalipa mabaya badala ya mema." Siku zile watu walisaidiana, hukuweza kuwa na chakula na mwingine ana njaa! Tukumbuke maagizo katika Waebrania kwamba tusiache kuwakaribisha wageni au kusaidia wenye shida, kwani wengine wamekaribisha malaika bila kujua.

Daudi akaapa akisema, "Mungu awafanyie adui za Daudi na kuzidi, nikiwaachia katika wote walio wake hata mtoto mume mmoja, kutakapopambazuka asubuhi." Ndipo Abigaili alifanya haraka kushuka kwenye punda wake na kuanguka kifudifudi akainama mpaka nchi miguuni pa Daudi na kusema kwa hekima; "bwana wangu, juu yangu mimi na uwe uovu; tafadhali mjakazi wako na anene masikioni mwako, nawe uyasikilize maneno ya mjakazi wako. Nakusihi bwana wangu, wewe usimwangalie mtu asiyefaa, yaani, Nabali na upumbavu wake; lakini mimi mjakazi wako, sikuwaona hao vijana wa bwana wangu, aliowatuma." Akamwambia amekuja kumzuia asimwage damu na kujilipiza kisasi mwenyewe, aache Mungu afanye hiyo kazi. "Basi sasa adui zako, na hao wamtakiao bwana wangu mabaya wawe kama Nabali." Akamwambia apokee zawadi alizomletea na kusamehe makosa yote, maana BWANA atafanya nyumba yake kuwa imara kwa sababu anapiga vita vya BWANA na uovu usionekane ndani yake. Akamsihi amkumbuke BWANA atakapokuwa amemtendea mema na ametawazwa kuwa mfalme wa Israeli, ila asimwage damu bure bali aache Mungu alipize kisasi. Daudi akamshukuru Abigaili akisema, "Ahimidiwe BWANA Mungu wa Israeli aliyekuleta unilaki, na busara yako ili nisimwage damu, na kulipiza kisasi mwenyewe." Akapokea vitu mikononi mwa Abigaili, na kusikiliza sauti yake. Abigaili japo aliolewa na mume asiyejali watu, lakini alijua jinsi ya kuishi naye. Hata nasi tukimjua mtu alivyo, tutajua kuishi naye

kwa hekima ya mbinguni na uvumilivu kama Abigaili, na kutunza amani.

Abigaili alirudi na kukuta Nabali amefanya karamu ya kifalme na moyo wake ulifurahi, na akalewa. Abigaili hakusema cho chote akingoja kupambazuke. Ikawa asubuhi ulevi ulipomtoka, Abigalili akamweleza hayo yote, na moyo wake ukafa ndani yake akawa kama aliyeshikwa ganzi au kupooza. Baada ya siku kumi Nabali akafa. Watumishi wa Daudi walitumwa kumwendea Abigali naye akamposa na kumwoa. Abigaili akaona amepata kibali kuolewa na mtumishi wa Mungu. Kisha Daudi akamwoa Ahinoamu wa Yezreeli.

Ombi: Hebu Bwana  awape wote walio katika ndoa au familia zenye changamoto kama hizo ujasiri wa kustahimili hadi ukombozi utakapokuja, ikiwezekana kupitia uongofu wa mwenzi mwenye shida ya kitabia. Wale wanaofuata maelekezo ya Mungu hawatashindwa kamwe. Hakika tunapaswa kushirikiana na Yule ambaye hajui kushindwa.

*Wazazi waombe Mwongozo wa MUNGU—Wazazi, nyenyekezeni mioyo yenu mbele za MUNGU. Anza kazi kamilifu kwa watoto wako. Msihi Bwana akusamehe kulipuuzia kwako Neno Lake katika kutojali kuwazoeza watoto wako katika njia wanayopaswa kuiendea. Omba nuru na mwongozo, dhamiri nyororo, na maamuzi/ utambuzi ulio wazi ili uone makosa na kufeli kwako. MUNGU atasikia maombi kama hayo kutoka kwenye moyo mnyenyekevu na uliopondeka


---

Nabali ina maana gani? Mtumishi alimwambiaje Abigaili kuhusu Daudi? Abigaili alitumia hekima gani kuondoa maafa nyumbani mwake? Je, Nabali alikufaje? Kwanini Yesu tu ndiyo mfano wa kuigwa katika kila kitu na si Daudi?

**SIKU YA 84**
**(Machi 24)**

# Sauli Amwinda Tena Daudi

**- 1 Samweli 26-28**



Wazifi walimwendea Sauli kule Gibea, ili wamfurahishe mfalme; japokuwa walijua mfalme ni mwovu, na hatendi haki. Wakamwambia, "Daudi amejificha kwenye kilima," basi Sauli naye akaondoka akishuka nyikani Zifu na watu 3000. Japo alikuwa mfalme na mwenye nguvu na utajiri, alihangaika kwa wivu na chuki. Alienda kumtafuta Daudi, kisha akapiga hema kwenye kilima cha Hakila, na Daudi alikuwa ametuma wapelelezi na hajajua Sauli alikuwa amekwisha fika. Akaenda pale alipotua Sauli na kupaangalia. Sauli na Abneri, mwana wa Neri, jemadari wake wa jeshi walikuwa hapo. Akaona Sauli amelala kati ya magari; na wanajeshi wamepiga hema wakimzunguka na kulala fofofo. Akamwambia Ahimeleki, Mhiti na Abishai, mdogo wa Yoabu aliyekuwa mpwa wa Daudi waende kwa Sauli kambini. Wakaona fumo la Sauli limechomewa chini, karibu na kichwa chake. Ndipo Abishai akamwambia Daudi, "Mungu amemtia adui yako mikononi mwako leo, basi niache nimpige kwa hilo fumo…pigo moja, sitampiga mara ya pili." Daudi akamkataza asimwangamize, kwani ni masihi wa BWANA, "Siku yake itampata, atashuka kwenda vitani na kupotea. Hasha nisiunyoshe mkono wangu juu ya masihi wa BWANA." Bali walitwaa fumo na gudulia la maji wakaenda, bila mtu kuwaona, wala kujua au kuamka, kwani walikuwa na usingizi mzito kutoka kwa BWANA.

Daudi alienda ng'ambo ya pili na kusimama kwenye kilima akiacha nafasi tele kati yao, na akapiga kelele kumwita Jemedari Abneri. Abneri alishtuka na kusema, "U nani wewe unayemlilia mfalme?" Naye Daudi akajitambulisha na kusema, Abneri ni shujaa na hakuna kama yeye katika Israeli, ila kuna mtu

aliingia ili kumwangamiza mfalme bwana wake naye haukutenda vyema, kwani hakumlinda mfalme. “Umestahili kufa kwa sababu hukumlinda bwana wenu mfalme.” Akawaonesha gudulia la maji na fumo la mfalme. Sauli alitambua sauti ya Daudi na kusema tena, “hii ndiyo sauti yako Daudi mwanangu?” naye Daudi aliitika ndiyo, bwana wangu mfalme. Na akamwuliza mfalme kwa nini anamwinda hivi, kwa uovu gani, “isianguke damu yangu chini, mbali na uso wa BWANA maana umetoka kutafuta uhai wangu kama vile mtu awindavyo kware mlimani.” Sauli akakiri amekosa, na kumwambia Daudi arudi, na hatamdhuru tena, kwa kuwa maisha yake yalikuwa ya thamani machoni pake, “nimetenda upumbavu, nimekosa sana.” Alikuwa anaungama ila haachi uovu, hata leo tujihadhari na kutobadili mienendo yetu baada ya kutubu. Daudi akamwambia kijana mmoja avuke atwae fumo, “Naye BWANA atamlipa kila mtu haki yake, na uaminifu wake; maana BWANA amekutia mikononi mwangu leo” nami nilikataa kumdhuru masihi, na kama vile maisha yako yalivyokuwa na thamani machoni pangu, maisha yangu na yawe na thamani machoni pako. Sauli akamwambia Daudi abarikiwe, atatenda mambo makuu, tena hakika yake atashinda. Basi Daudi akaenda zake; na Sauli naye akarudi kwake. Huu ndiyo ulikuwa mwisho wa kuonana kwao.

Safari hii Daudi akaamua aende mbali kwani alijisemea moyoni mwake, “siku moja nitaangamia kwa mkono wa Sauli,” hivyo jema ni kukimbilia kwa Wafilisti, ili Sauli akate tamaa kwa habari yake asimfuate tena mipakani mwa Israeli. Daudi akaenda na watu 600 na akamwendea Akishi, mfalme wa Wafilisti na kukaa huko. Sauli alipata habari kwamba Daudi amekimbia Gathi, wala hakumtafuta tena. Daudi akamsihi kama ni vyema Akishi ampe mji na shamba akae, na si katika nyumba ya kifalme. Akapewa Siklagi, nao ukawa mji wa wafalme wa Yuda. Akaa kule mwaka na nusu hivi na watu wake, na wakawa wakishambulia, Wageshuri, Wagirizi, na Waamaleki. Akirudi kwenye mashambulizi mfalme alimwuliza aliposhambulia naye alisema alikuwa anashambulia Israeli. Hakuhifadhi mtu kuleta ushahidi Gathi. Akishi akamsadiki Daudi na kusema “amewachukiza kabisa adui” wa Wafilisti, kwa hiyo “atakuwa mtumishi wangu hata milele.” Daudi hapa alifikia hatua kama ile ya Eliya alipokimbia kwenye mlima wa Bwana kwaajili ya uovu wa Yezebeli. Wakati binadamu, tunatindikiwa na imani yetu ikapunguka, ni vyema kufarijiana na wengine na kuzisoma ahadi za Mungu. “Naam, na wote wapendao kuishi utauwa katika Kristo Yesu watateswa.” 2 Tim. 3:12. Tunapokata tamaa, tuepuke kuchukua maamuzi bila kushauriana na Mungu. Tunaweza kufikiria hatua tunayochukua ndiyo suluhisho pekee, lakini tunaweza kuwa tumekosea, kwani mipango yetu inaweza isipatane na Mungu kwetu. Kwa mfano, mtoto wa Mungu ambaye amekuwa akitafuta kazi bila kuipata anaweza kuamua kuhamia nchi zilizoendelea. Huenda kusiwe na kosa katika kufanya hivyo, ila uamuzi huo ni hatari ukichukuliwa bila kushauriana na Mungu. Wengi wamehamia huko ili tu kujipatia mahitaji ya msingi au kujikimu kiuchumi na wamekumbana na changamoto ambazo zimetweza imani zao na wanafamilia majumbani mwao. Hivyo, hata iweje, shauriana na Mungu sikuzote na usadikishwe kuhusu mapenzi Yake kabla hujachukua hatua yoyote maishani. Mungu ameahidi, akisema, “Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; nitakuongoza kwa jicho Langu.” Zaburi 32:8. Mungu hasemi uongo. Bali Anasema tu kile atakachofanya. Atakuongoza leo ukimruhusu!

Ikawa Wafilisti walikusanya majeshi ili kupigana na Israeli, naye Akishi akamwambia Daudi waende naye, na jeshi lake, naye atamlinda mfalme wa Wafilisti. Daudi akasema vyema, ila moyoni alipata hofu kwamba sasa atapiganaje na watu wake.

Samweli alikuwa amefariki na Sauli alikuwa amewaondolea mbali hao wenye pepo wa utambuzi na wachawi katika nchi kutokana na Amri ya Mungu. Wafilisti wakakusanyika Shunemu naye Sauli akakusanya Waisraeli huko Gilboa, na alipoona majeshi ya Wafilisti aliogopa, na moyo wake ukatetemeka sana, na alipouliza kwa BWANA, hakujibiwa wala kwa ndoto wala kwa Urimu wala kwa manabii. Ndipo Sauli akawaambia watumishi wake wamtafute mwanamke mwenye pepo wa utambuzi, apate kuulizia kwa wafu vita hii. Mwanamke huyu aliishi Endori. Basi Sauli akabadilisha mavazi yake ya ufalme na jeshi aende kama raia wa kawaida na wakamfikilia mwanamke huyu mchawi usiku. Akamwambia "Tafadhali unibashirie kwa utambuzi, ukanipandishie yeye nitakayemtaja kwako." Mwanamke huyu akamwambia Sauli "mfalme aliua watu wenye pepo wa utambuzi na wachawi katika nchi, mbona basi wanitegea tanzi uhai wangu, ili kuniua." Sauli akamwapia kwamba haitampata adhabu yoyote kwa jambo hilo. Ndipo yule mwanamke alipouliza, anataka amlete nani aliyekufa?

Lazima tujue kwamba hakuna mchawi anayeweza kumleta mtu, toka kwa wafu, vinginevyo, watu wote wangeleta wapendwa wao. Hakuna roho inayoelea yenyewe bila mwili. Mavumbi + pumzi ya uhai (roho)= Mtu hai. Mwili hauwezi ukaishi wenyewe na kutenda mambo, na roho au pumzi ya uhai haiwezi kuishi yenyewe. Nabii wa Mungu alikuwa amekufa. Nguvu hiyo itendayo miujiza (ya adui) ambayo inajidhihirisha kupitia katika ile Imani ya umizimu itaweka upinzani wake dhidi ya wale wanaochagua kumtii Mungu kuliko wanadamu. Ujumbe kutoka kwa mizimu (hayo mapepo) utatangaza kwamba Mungu amewatuma na kusema mambo fulani ambayo ni ya uongo, kama katika kesi hii. Basi Sauli akasema, "Samweli", na yule mwanamke mwenye pepo alipomwona pepo aliyejileta kama Samweli, alilia kwa sauti kuu na kumwambia Sauli "mbona umenidanganya? Kwa kuwa wewe ndiwe Sauli." Mfalme akamwambia asiogope, na akamwuliza anaona nini? Na yule mwanamke akamwambia Sauli, "Naona mungu anatoka katika nchi." Tunapenda kukazia kwamba, huyu hakuwa Samweli, bali pepo mbaya aliyejibadilisha aonekane kama mtu fulani kutoka kwa wafu. Sauli akauliza, ni mfano wa nini? Akajibu ni "mzee anazuka, naye amefunikwa vazi." Basi akatambua kuwa ni Samweli na akainama uso na kusujudu. Ndipo ule mfano wa Samweli au mzimu ulipozungumza na kumwambia, "Mbona umenitaabisha mimi, hata kunipandisha juu?" Sauli hakumwona Samweli, aliamini tu yale maneno ambayo mchawi alimwambia. Akifikiria atapata habari njema, alishangaa akigombezwa na kupewa habari mbaya. Sauli akajitetea kwamba ametaabika sana, kwa kuwa Wafilisti wanamjia Naye Mungu "ameniacha, hanijibu tena, wala kwa manabii, wala kwa ndoto; kwa hiyo nimekuita wewe, ili unijulishe, nifanyeje." Ule mzuka wa Samweli ukasema, kwa nini amwulize yeye, ikiwa BWANA amemwacha, "naye amekuwa adui yako?" BWANA amekurarulia ufalme wako na kumpa jirani yako, yaani, Daudi kwa sababu wewe hukuitii sauti ya BWANA, wala hukutimiza hasira Yake na kuwaua Waamaleki waliokuwa waovu mno. Sauli alitoka pale amechanganyikiwa zaidi, amekata tamaa ya vita kabisa, na mahusiano yake na Mungu yalikuwa yamekwisha.

Watu wengi sana ulimwenguni leo wanadanganywa kwamba roho yenye ufahamu hutoka ndani ya mwili mtu anapokufa na kwenda mbinguni au motoni. Kupitia umizimu, wengine huwasiliana na roho hizi. Watu hawa hawawasiliani na roho za jamaa yao aliyekufa, bali na malaika aliyeanguka toka mbinguni, ambaye hutengeneza wafu bandia. Kwa njia hii, Shetani anaendeleza uwongo aliomwambia Hawa katika bustani ya Edeni kwamba hakika hatakufa kama utakula tunda lililokatazwa (Mwanzo 3:1-6). Sasa kwa kuwa tunakufa, anatudanganya kwamba hatujakufa kiukweli, bali tunaishi katika ulimwengu wa roho kama nafsi. Shetani ni mwongo na baba wa huo uongo (Yohana 8:44).

Wale wote wanaoamini kwamba kuna nafsi inayoukimbia mwili wakati wa kifo na kwenda mbinguni au kuzimu wanatayarishwa kwa ajili ya udanganyifu mkuu wa Shetani utakaotangulia ujio wa pili wa Yesu. Udanganyifu mkuu huu utasababisha kupotea kwa wote wanaoukubali. Mungu atuangazie sote binadamu ili tuepuke kudanganywa.

*Wale walio tayari Kuongozwa Wanaweza Kujua Mapenzi ya MUNGU— Bwana hufunua mapenzi Yake kwa wale walio na bidii ya dhati na wanaotamani kuongozwa Naye. Sababu ya kukosa kwako ufanisi ni kwamba umeacha wazo la kujua na kuyafanya mapenzi ya MUNGU, na hivyo haujui chochote katika mtazamo chanya. Kwa nini Wazifi walimwambia Sauli Daudi alipo? Kwa nini Daudi alisema ilimpasa Abneri afe? Kwa nini Daudi alienda kwa Akishi? Kwa nini Sauli alipata hofu na kutetemeka? Kwa nini ule mzuka wa Samweli haukuwa Samweli mwenyewe? Je, kwa nini ni dhambi kwenda kwa wenye pepo wa utambuzi au wachawi? Kwa nini watu huamini kwamba mtu aliyekufa anawatembelea toka kuzimu? Umizimu maana yake ni nini?

**SIKU YA 85**
**(Machi 25)**

# Mchawi wa Endori

**- 1 Samweli 29-30**



Akiwa bado kwa mwanamke mwenye pepo wa utambuzi kule Endori, Sauli aliambiwa na ule mzimu ambao ulikuwa mfano wa Samweli, kwamba, "BWANA atawatia Israeli mikononi mwa Wafilisti, na hata kesho yeye na wanawe watakuwa kuzimu." Sauli alianguka kifudifudi na kuingiwa na hofu kwa sababu ya maneno ya mzuka ule wa Samweli, wala hakuwa na nguvu yoyote, kwa vile alikuwa hajala mchana kutwa na usiku pia. Yule mwanamke mwenye pepo akamwendea Sauli kwa vile aliona anataabika, na kumsihi kwamba amehatarisha maisha yake ili afanye anachotaka, na sasa yeye asikilize sauti yake kwa kukubali atengeneze mkate ili ale na kupata nguvu kisha aende zake. Sauli akakataa kula, ila watumishi wake pamoja na yule mchawi wakamlazimisha naye akawasikiliza. Sauli akainuka na kukaa kwenye kitanda, na yule mwanamke akamchinjia ndama aliyenona na akakanda mkate wa mofa na kumwandalia na watumishi wake nao wakala; na kwenda zao usiku ule.

Ni muhimu kujua kwamba aliyekuja kuzungumza na Sauli sio Samweli, bali ni

Shetani aliyejigeuza awe mfano wake. Hata wengi siku hizi wanafanya ibada za wafu, na kuita ndugu zao waliokufa na Shetani hujigeuza na kuzungumza nao. Neno la Mungu linasema mtu akifa, amekufa, na anangoja hukumu. Yeyote anayetokewa na mtu aliyekufa ni mbinu za Shetani. Shetani anao uwezo wa kufanya maajabu. Tujihadhari maana nchi zingine kama Marekani ibada hizi za wafu zilianza toka zamani na kuna makuhani wengi wa ibada za wafu wanaolipwa ili wawatokezee watu wapendwa wao. Endapo umefiwa na yule aliyekufa akakutokea, ujue kwamba ni malaika wa Shetani wala si ndugu au jamaa yako aliyekufa, kwani wafu hawajui neno lolote.

Vitabu, sinema, na programu za televisheni zote zimeendeleza wazo kwamba tunapokufa, tunaingia katika hali nyingine ya ufahamu. Kosa hili linatangazwa katika mimbari nyingi za Kikristo vile vile. Hata sayansi imehusika. Kuna taasisi nchini Marekani unaojaribu kuunda teknolojia ambayo, inadai, itatuwezesha kuwasiliana na wafu, ambao wanaamini bado wako hai lakini wanaishi "baada kufa/PMP." Kwa kuwa kosa hili limeenea sana, haitashangaza kuwa udanganyifu huu utakuwa na jukumu muhimu katika matukio ya mwisho ya historia ya binadamu. Je, uwongo huu unadhihirishwa kwa njia gani katika utamaduni wako mwenyewe? Kwa nini ni lazima tutegemee Neno la Mungu kuliko yale ambayo hisia zetu zinatuambia?

Basi Wafilisti walikusanyika na jeshi lao huko Afeki na Waisraeli wakakaa kwenye chemchemi ya Yezreeli, na viongozi wa Wafilisti walipita kwenye gwaride maelfu, elfu na Daudi na watu wake walipita mwishoni wakiwa upande wa Wafilisti na mfalme Akishi. Ndipo wakuu wa Wafilisti walipomwona Daudi waliuliza, 'hawa Waebrania wanafanya nini hapa." Akishi akajibu "huyu Daudi, yule mtumishi wa Sauli, mfalme wa Israeli, ambaye amefuatana na mimi siku hizi, naam, miaka hii, wala mimi nisione hatia kwake, tangu hapo aliponiangukia mimi hata leo?" Lakini wakuu wa Wafilisti wakakasirika, wakaona atawasaliti, na wakamwambia Akishi "mrudishe huyu apate kurejea mahali pake ulipomwagiza, ili asiende pamoja nasi vitani asije akawa adui wetu vitani." maana atajipatanisha na bwana wake Sauli kwa njia hiyo. Wakamwambia Akishi mtu huyu ni Jemedari kwani wanakumbuka alivyosifiwa kwamba ameua makumi elfu na Sauli elfu tu. Basi Akishi akimpenda Daudi akamwita, na kumwambia kwamba yeye amekuwa mwaminifu, tena ametoka na kuingia kwa uadilifu, na wala "sikuona uovu ndani yako tangu siku ile uliponijia hata leo. Ila wakuu Wafilisti hawataki wewe uende nasi, "basi urudi, uende zako kwa amani, ili usiwachukize hao mashehe wa Wafilisti." Daudi akasema, "Lakini mimi nimefanyaje? Nawe umeona nini kwangu mimi mtumwa wako, muda wote niliokaa mbele yako hata leo, nisipate ruhusa niende na kupigana na adui za bwana wangu mfalme? Akishi akamhakikishia kwamba yeye ni mwema, na hana shida machoni pake, ila hao wakuu wamekataa asiende nao vitani. Akamsihi aamke asubuhi na mapema na yeye na watumwa wake na kwenda zao.

Daudi alifanya mambo kwa makosa kama sisi tunavyofanya wakati mwingine. Wakati fulani alipata ushindi kwa kumwamini Mungu. Ila wakati mwingine alishindwa kwa kutomwamini. Bwana daima ni Mwenye huruma kwa wale ambao mioyo yao imetolewa Kwake. Mungu huweza kuwaokoa hata wale walioingia katika magumu kwasababu ya makosa yao wenyewe. Haijalishi mahangaiko au

majaribu unayoyapitia, mweleze jambo lako Bwana. Na roho yako itaimarishwa kwa uvumilivu. Na kisha Njia itakuwa wazi kwako kujiondoa kutoka kwenye fedheha na shida. Kadiri unavyojijua kuwa wewe u dhaifu na kwamba huna msaada zaidi, ndivyo unavyozidi kuwa na nguvu katika nguvu Zake Bwana. Kadiri mizigo yako inavyozidi kuwa mizito, ndivyo unavayozidi kubarikiwa unapoitupa kwa Bwana, ambaye Ndiye Mbeba Mzigo wako.

Basi Daudi na jeshi lake waliamka asubuhi na kurudi nchi ya Wafilisti huko Yezreeli. Daudi akifika Siklagi, siku ya tatu alikuta Waamaleki wameshambulia Negebu na kupiga Siklagi na hata kuichoma moto. Daudi na watu wake walipoona mji umechomwa, na wake zao na watoto zao wamechukuliwa mateka, wakainua sauti na kulia, mpaka nguvu za kulia zikawakosa. Hata wake wawili wa Daudi, Ahinoamu na Abigaili walikuwa wamechukuliwa. Daudi alisononeka maana watu wa jeshi lake walitaka wampige mawe, kulipiza kisasi kwamba wana na binti zao wamechukuliwa. Lakini Daudi alijitia nguvu katika BWANA. Daudi akamwambia Abiathari alete naivera ya kuhani ili aulize kwa BWANA kama alifuate jeshi hili, na kama atawapata. Basi BWANA akamjibu awafuate na hakika atawapata, na kuwapokonya wote. Daudi akaenda na watu wake 600 na kufika kijito cha Besori ambapo wale walioachwa nyuma walikaa. Kutoka hapo watu 400 ndiyo walienda mbele maana watu 200 walichoka na wakataka kuzimia. Walimkuta Mmisri mmoja kwenye uwanja akiwa ameishiwa nguvu kwa njaa ya siku tatu. Wakampa maji, vipande vya tini na zabibu. Alipokula roho yake ikamrudia, na Daudi akamwuliza, kwamba yeye ni nani? Alijibu kwamba yeye ni mtumwa wa Mwamaleki ila ni Mmisri. Akasema "bwana wangu aliniacha kwa kuwa nilishikwa na ugonjwa." Akawaambia ni wao walishambulia Negebu na kuchoma Siklagi. Wakamwuliza kama anaweza kuwapeleka kule Waamaleki walipo? Akamsihi aape kwamba hatamwua au kumtia mikononi mwa bwana wake. Akawaongoza kulifikia jeshi, wakawakuta wametawanyika wakisherehekea kwa kula na kunywa zile nyara walizopata.

Daudi na jeshi lake waliwapiga hawa Waamaleki toka jioni mpaka kesho yake, hakuna aliyeokoka, ila vijana mia nne waliopanda ngamia na kukimbia. Wakawapokonya mateka waliochukuliwa na Waamaleki, hata wale wakeze wawili, na kurudisha vitu vyao vyote, hata zile nyara. Daudi akawafikia watu 200 waliotaka kuzimia, waliokaa kwenye kijito, nao walitoka kumlaki na kushangilia. Wengine kati ya wale 400 wakapata uovu na tamaa na kusema kuwa kwa kuwa wale watu 200 hawakwenda pamoja nao, hawatapata kitu katika nyara walizoteka isipokuwa wake na watoto wao, wawachukue hao na kwenda zao. Lakini Daudi akawasihi wasitende vile, kwani aliyewapa ushindi na nyara ni BWANA, Naye amewahifadhi na kulitia jeshi la Waamaleki mikononi mwao. Daudi akaweka sheria au amri katika Israeli ya "fungu lake yeye ashukaye vitani, ndivyo litakavyokuwa fungu lake huyo akaaye karibu na vyombo; watagawiwa sawasawa."

*Mtumaini MUNGU Naye Ataongoza Njia Yako — Wengi wanashindwa kupanga mipango dhahiri ya siku zijazo. Maisha yao hayajatulia. Wanashindwa kutambua matokeo ya mambo, na hii mara nyingi huwajaza wasiwasi na machafuko. Hebu na Tukumbuke kwamba maisha ya watoto wa MUNGU katika ulimwengu huu ni maisha ya safari ya hija (wasafiri na wapitaji). Sisi hatuna hekima ya kupanga

maisha yetu wenyewe. Sio juu yetu kutengeneza au kuyaumba maisha yetu ya baadaye. “Kwa imani Abrahamu alimtii MUNGU alipoitwa aende katika nchi ambayo MUNGU angempa iwe yake. Ingawa hakujua alikokuwa anakwenda, Abrahamu aliendа. Waebrania 11: 8.

---

Kwa nini yule aliyeletwa na mwanamke mchawi wa Endori hakuwa Samweli mwenyewe? Mungu alimwokoaje Daudi asiende kupigana vita na Israeli? Akishi alimwambiaje Daudi? Mmisri alilisaidiaje jeshi la Daudi? Ni sheria gani ya kugawana nyara iliwekwa katika Israeli?

**SIKU YA 86**
**(Machi 26)**

# Madanganyo ya Shetani

**- 1 Samweli 29 na 30**



Kutokana na mafundisho ya Biblia, mtu akifa hawezi kuwasiliana tena na wale walio hai wala hatarudi nyumbani mwake. Ayubu 7:8-10. Kuzungumza na wafu si fundisho la Neno la Mungu. Biblia inasema, "kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote, wala hawana ijara tena, maana kumbukumbu lao limesahauliwa." "… kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe." Mhubiri 9:5,10. Tena mtu akifa haendi mbinguni moja kwa moja. Aliyekufa hajui neno lolote, hukaa kaburini mpaka YESU atakapokuja kufufua wafu. Soma maandiko kuhusu ufufuo. Mtu lazima afufuliwe ili aishi tena na kuwa mbinguni. Watu wawili waliokufa na wako mbinguni kutokana na Biblia ni Musa na YESU. Na waliochukuliwa mbinguni bila kuonja mauti ni Henoko na Eliya. Hakuna roho inayoishi bila mwili, maana udongo + pumzi ya uhai= ndiyo binadamu, Mafundisho mengi husema kwamba mtu akifa roho yake huenda mbinguni au Jehanamu naye huzikwa kaburini, na roho hiyo ikiwa peke yake ina ufahamu! Hili si fundisho la Biblia, maana nafsi hai ni mwili na roho, roho haiwezi ikaishi peke yake bila mwili na akawa mtu au nafsi hai, kama Adamu au Hawa na mwili hauwezi kuishi pekee yake na ikawa nafsi hai. Hili linapaswa kuchunguzwa kwa kulinganisha mafungu ya Biblia kuanzia Mwanzo

mpaka Ufunuo, na sio kuchukua fungu moja tu na kuhitimisha.

Watu wengine, kama dini ya Hindu wanaamini mtu akifa anazaliwa kuwa kiumbe kingine kutokana na aliyofanya akiwa hai, mfano, akiwa mwema kwa watu atazaliwa kama mfalme tajiri, na akiwa mbaya na mkatili, atazaliwa kama mbwa au konokono mahali pengine, kutegemeana na uovu au wema wake.

Je, Sauli alimwona na kuzungumza na nani siku ile kwa mchawi wa Endori? Sauli alikuwa anawasiliana na Shetani, aliyejibadilisha na kuchukua umbo la Samweli. Malaika wa giza wanaweza kujibadilisha na kuwa kama yule mpendwa aliyekufa, inabidi tuwe makini. Mungu alimwumba mtu na kumpulizia pumzi ya uhai. Katika kifo hakuna kumbukumbu, maumivu au huzuni.

Pengine hili ni jambo zuri, kwani kama wafu wangeweza kuwa na kumbukumbu na fahamu ya kuona yanayotokea duniani, basi wangekuwa na huzuni nyingi kwa wale watu waliowaacha. Hata hivyo watu waliofufuliwa na Yesu kama Lazaro hawakushuka kutoka mbinguni, bali walitoka makaburini mwao . Lakini Yesu akirudi makaburi yatafunguliwa (1Wakorintho 15). Kwanini makaburi yafunguliwe na watu walishaenda mbinguni basi. Kifo hichi tunachokufa kama Lazaro ni kifo cha kwanza. Ila YESU arudipo na kufanya hukumu, wale waliotenda uovu na machukizo kwa kupinga maagizo ya MUNGU na kutotubu dhambi zao watapata adhabu ya kifo cha pili, hiki ni kitakuwa kifo cha milele, hakuna ufufuo tena kwao. YESU alikufa kwaajili yetu kifo cha pili, ili tusife milele.

Shetani anajaribu kudanganya watu, na hivyo ni muhimu tusiamini wabashiri, wachawi, na wenye pepo wa utambuzi. Usikubali kuongea na mtu ambaye alikufa na sasa inasemekana “amerudi” bali mkemee kwa Jina la Yesu. Wacheza filamu kadhaa huonesha picha za filamu za watu waliokufa na wakawatokea ndugu zao. Filamu si kitu halisi, nyingi zina mafundisho ya uongo. Siku hizi hakuna filamu inayouza vyema isipokuwa na mambo ya uchawi. Paulo alisema “Lakini ndugu hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika, kama na wengine wasio na matumaini. Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja Naye.” Parapanda italia na makaburi yatafunguka na wafu watatoka kwenye makaburi, wengine wataondoka kwa ufufuo wa uzima na wengine ufufuo wa mauti.

Kwenda kutafuta wanajimu, wapiga ramli, na wachawi ili kusaidia shida zetu kama za kupandishwa vyeo, mtoto kuumwa, kujua ya mbeleni, kupotea kwa ndugu, au kupata kazi ni makosa. Kama tunataka msaada wowote tumwombe Mungu Mwenyewe moja kwa moja Naye atatusaidia. Na kama kuna mashirika ya serikali kama polisi, au ushauri/nasaha basi pia yatumiwe kwa mambo fulani.

Hebu tumwombe Mungu atufunulie, na atusaidie ili tusiingie kwenye shida kama ya Sauli, maana alipoenda kwa mchawi wa Endori, haikumsaidia kutatua tatizo. Watu wengi siku hizi wamekutana na sura wanazofikiri ni za ndugu au marafiki zao walioaga dunia. Mwonekano au sura zao wanazitambua, na maneno na sauti ni kama ya yule aliyekufa. Ila ni mtu bandia tu yaani mzimu. Wengi wanafarijiwa

na uhakikisho kwamba wapendwa wao wanafurahia huko mbinguni, na kumbe ni "roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." Tujikabidhi kwa Mungu ili uwe salama mikononi Mwake.

*Yachunguze Maandiko kwa Sala kwa ajili ya Uongozi wa Bwana — Wale ambao hawataki kukubali ule Ukweli ulio wazi, unaokatakata, na ulio thabiti wa Biblia, daima wakaendelea kutafuta hekaya za kupendeza ambazo zitatuliza au kunyamazisha dhamiri zao. Kadri ya mafundisho yanavyokuwa na upungufu wa mionjo ya kiroho, kujikana nafsi, kujidhili au kujinyenyekeza, ndivyo yanavyopokelewa kwa upendeleo mkubwa zaidi. Watu hawa wanapunguza nguvu za kiakili kutumikia tamaa zao za mwili. Hujiona wenye busara sana katika mawazo yao wenyewe yenye kiburi hata wasitafute Maandiko na kutubu kwa roho na maombi ya moyo uliopondeka na maombi dhati kwa ajili ya mwongozo wa Bwana, hawana ngao dhidi ya udanganyifu. Shetani yuko tayari kutimiza matamanio ya moyo wao, naye anaingiza udanganyifu wake alioushika mkoni mwake mahali pa ile Kweli na hivyo kuwatawala kirahisi sana.

---

Je tunaweza kuzungumza na mtu aliyekufa? Je Mtu akifa huenda wapi? Je! Roho inaweza kuwa nafsi hai bila mwili ikaishi peke yake na kuelea angani akawa mtu au nafsi hai? Kwanini makaburi yatafunguliwa Yesu ajapo? Soma zaidi kitabu kinaitwa Pambano Kuu Sura ya 34 kuhusu umizimu.

SIKU YA 87
(Machi 27)

# Kifo cha Sauli

**- 1 Samweli 30-32 Samweli 1-3, 1 Mambo ya Nyakati 10**

Wafilisti wakapigana na Israeli na watu wa Israeli wakakimbia mbele yao, wakaanguka watu wengi katika mlima wa Gilboa. Sauli kwa vile alikuwa jitu refu, ikawa rahisi kwa Wafilisti kumwona wakamfuata na kumwua na wanawe Yonathani, Abinadabu na Malkishua. Vita vikawa vikali kwa Sauli na wapiga upinde wakampata na kumlenga, naye akafadhaika kwa jeraha hilo na akamwita mchukua silaha wake ili amwue na kummaliza, wasije wakamsimanga watu wasiotahiriwa kuwa wamemwua, lakini mchukua silaha alikataa akiogopa kumwua mfalme au mpakwa mafuta. Basi Sauli alitwaa upanga wake akauangukia na hivyo kujiua mwenyewe. Alijua kama Wafilisti wangempata pengine wangemtesa kwa ukatili mkubwa. Mchukua silaha alipoona bwana wake amekufa, naye alichukua upanga wake na kuuangukia, na hivyo kufa pamoja na Sauli. Siku zile ulikuwa ukimlinda mfalme akifa, unakufa pamoja naye kwani ungeonekana kwamba hukumlinda mfalme. Hivyo Sauli akafa na wanawe watatu siku iyo hiyo. Watu wa ng'ambo ya Yordani walipoona Waisraeli wamekimbia, nao wakakimbia na kuacha miji yao, na Wafilisti wakaenda na kukaa humo.



Siku ya pili Wafilisti walipokuwa wakiteka nyara waliona miili ya Sauli na watoto wake imeanguka kwenye mlima wa Gilboa na wakakata kichwa cha Sauli na kumvua silaha na kupeleka ujumbe kwa watu wao na miungu yao. Wakaweka silaha zake kwenye nyumba za miungu yao, na kutundika mwili wake huko. Jambo hili ni baya, kwani tai na wanyama wanaweza kuja na kuishambulia miili hiyo. Wenyeji wa Yabesh-Gileadi waliposikia waliyomtendea Sauli, mashujaa wao walienda usiku kucha na kuuchukua mwili wa Sauli na wanawe na wakaja kuizika, na kufunga siku saba. Kweli kutii ni bora kuliko dhabihu, tunapokosa, tuombe msamaha na kuacha njia zetu mbaya. Sauli hakuacha, alilia machozi na kusikitika, bali aliendelea na uovu. Biblia inasema alikufa kwa sababu ya kosa lake la kutoshika Neno la BWANA. Basi Sauli akauawa na ufalme akapewa Daudi. Mwisho wa wakati kutakuwa na mambo mawili tu, Kumwambia Mungu Mapenzi Yako yatimizwe, au Yeye kutuambia mapenzi yetu yatimizwe. Je, wewe unachagua lipi kati ya haya mawili?

Daudi alingoja kwa uvumilivu, akiwa mapangoni na kwenye hatari zingine. Baada ya kufa kwa Sauli, Daudi akitoka Siklagi, akaja mtu kutoka kambi ya Sauli na nguo zake zimeraruliwa akiwa amejaa mavumbi kichwani. Alipofika kwa Daudi alianguka chini na kusujudu, Daudi alipomwuliza anatoka wapi, alisema ameokoka katika vita vilivyokuwa vinaendelea, alikuwa kwenye kambi ya Waisraeli. Daudi akamwuliza vita ilikwendaje, naye akajibu, "watu wamekimbia vitani, tena watu wengi wameanguka na kufa; hata Sauli na Yonathani mwanawe wamekufa." Daudi akamwulizaje amejuaje Sauli amekufa? Ndipo yule kijana akasema uongo akifikiri atazawadiwa. Alisema alikuwa kilima cha Gilboa na Sauli alikuwa ameegemea fumo lake, magari ya farasi yakimfuatia kwa kasi' naye alipotazama nyuma, "Sauli akaniita, Nikajibu, mimi hapa," "Akaniambia, u nani wewe?" Nikamjibu, Mimi ni Mwamaleki. Mwamaleki huyu akasema kwamba Sauli alimwambia amepata shida na kupigwa mshale, na roho yake i ndani yake, basi akamwomba amwue. Naye yule Mwamaleki alisema, "Basi nikasimama karibu naye, nikamwua, kwa sababu nilijua hakika hawezi kupona baada ya kuanguka; kisha nikatwaa ile taji iliyokuwa kichwani mwake, na kikuku kilichokuwa mkononi mwake, nami nimevileta hapa kwa bwana wangu." Kijana huyo alifikiri kuwa Daudi atampongeza kwa kumwua adui yake, pengine ampe nafasi kwenye serikali yake, hakujua kwamba hata Daudi mwenyewe japo alifanyiwa unyama hakunyosha mkono wake kumwua masihi wa BWANA. Mtu huyu alikuwa mwongo kwani Sauli alijiua mwenyewe kwa upanga wake. Hii inatufundisha kuwa uongo si kitu kizuri kamwe. Basi Daudi alirarua nguo zake, na watu waliokuwa pamoja naye kwa kuomboleza na wakafunga hata jioni kwa ajili ya Sauli, na nyumba ya Israeli, na Yonathani mwanawe aliyekuwa rafiki wa karibu wa Daudi.

Naye Daudi akamwuliza yule kijana aliyempa habari, kwamba anatoka wapi akaeleza kwamba ni Mwamaleki. Akamwuliza, "jinsi gani haukuogopa kuunyosha mkono wako umwangamize masihi wa BWANA?" Ndipo Daudi akamwambia kijana wake amwendee na kumwangukia, basi akapigwa na kufa. Daudi akamwambia, "Damu yako na iwe juu ya kichwa chako mwenyewe, maana umejishuhudia nafsi yako ukisema nimemwua masihi wa BWANA." Daudi akamwomboleza Sauli na Yonathani na wanawe kwa wimbo huu, "Jinsi mashujaa walivyoanguka. Msiyahubiri mambo haya katika Gathi… wasije wakashangilia binti za Wafilisti. Sauli na Yonathani walipendwa na kupendeza Maishani wala mautini hawakutengwa; walikuwa wepesi kuliko tai. Walikuwa hodari kuliko simba. Enyi binti wa Israeli, mlilieni huyu Sauli ambaye aliwavika mavazi mekundu kwa anasa, akazipamba nguo zenu za dhahabu … Nimesikitika kwa ajili yako Yonathani ndugu yangu, ulikuwa ukinipendeza sana; upendo wako kwangu ulikuwa wa ajabu … Jinsi mashujaa walivyoanguka, Na silaha za vita zilivyoangamia."

Sauli angeweza kuwa mfalme mkuu, alikuwa na talanta nyingi nzuri, ila hakuwa na utii kwa Mungu na wivu ukamharibia maisha yake. Wivu huu ukamsumbua kwa kuleta pepo wachafu waliomtesa. Kwa vile aliacha kumtii Mungu alianza kupata mashauri toka kwa nguvu za giza, badala ya nguvu za Mungu. Daudi kwa upande mwingine alipenda kuwatendea maadui zake wema, hakufurahi aliposikia Sauli amekufa.

Daudi alitafuta ushauri kwa BWANA, akasema, “Niupandie mji wowote wa Yuda.” BWANA akamwambia, Haya! Panda. Daudi akasema, niupandie mji upi? Akasema “Hebroni.” Basi Daudi akapanda huko pamoja na wakeze wawili na watu waliokuwa pamoja naye, na wakakaa katika mji wa Heborni. Watu wa Yuda wakaenda kumtia Daudi mafuta kule awe mfalme juu ya nyumba ya Yuda kwa miaka saba. Daudi akatuma ujumbe kwa Yabesh-Gileadi waliomtendea Sauli fadhili na kumzika. “BWANA Naye sasa awatendee ninyi fadhili na kweli…mikono yenu itiwe nguvu, nanyi iweni mashujaa; maana Sauli bwana wenu amekufa, tena nyumba ya Yuda wamenitia mimi mafuta niwe mfalme juu yao.” Basi Abneri mwana wa Neri amirí wa jeshi la Sauli alimtwaa Ishboshethi mwana wa Sauli wa miaka 40, na kumpeleka awe mfalme juu ya makabila mengine ya Israeli. Kukawa na wafalme wawili sasa, Daudi na Ishboshethi. Ishboshethi akatawala miaka miwili kati ya Israeli, lakini Yuda walienda na Daudi.

Yoabu aliyekuwa Jemadari wa jeshi la Daudi na mpwa wake, aliamua kukutana na Abneri wakatoka wakutane kwenye ziwa la Gibeoni, wakaketi kila jeshi upande mmoja ya ziwa. Yoabu akasema, “tafadhali vijana hawa na waondoke na kucheza mbele yetu.” Wakaondoka na kwenda watu kumi na mbili wa Benyamini na kumi na mbili wa Daudi. Wakacheza mchezo wa mapanga, Wakauana mashujaa 24 mahali hapa, kisha wengine wakaingilia mapambano na watumishi wa Daudi wakashinda. Michezo ya ukatili ipo hata leo, tunapaswa kuwa waangalifu sana kuiepuka kabisa michezo yoyote yenye mnuso wa ukatili, maana ni dhambi kubwa. Baadhi ya burudani maarufu, kama vile mpira wa miguu na ndondi, zimekuwa shule za ukatili. Zimekuza sifa sawa na ile michezo ya Rumi ya kale. Roho ya ushindani, kutawala wengine, kiburi katika nguvu ya ukatili, kutojali uhai ambao Mungu ametoa, vinafanya vijana wafanye mambo ambayo ni ya kutisha. Michezo mingine ya riadha, ingawa si ya kikatili sana, inakuwa ibada au miungu kwa wengi. Hii huchochea kupenda anasa na msisimko, na hivyo kukuza chuki kwa kazi za mikono ambazo zina manufaa, yaani huendekeza uvivu na mwelekeo wa kukwepa majukumu na wajibu katika utendaji wa kazi. Huharibu furaha na utulivu wa maisha. Mlango unafunguliwa kwa uasi, na kile kilichoanza kama jambo la kufurahisha, huwa cha kuogofya.

Basi Abneri akakimbia, na mpwa wa Daudi, Asaheli ambaye alikuwa ndugu wa Yoabu alimkimbilia kutaka kumwua, naye Abneri akamtahadharisha Asaheli aliyekuwa na wepesi; kwamba ageuke, na aache kumfuata, “kwa nini nikupige hata chini? Hapo ningewezaje kuinua uso wangu mbele ya Yoabu ndugu yako?” Lakini Asaheli hakugeuka, hivyo Abneri akampiga tumboni kwa ncha ya mkuki, naye akaanguka hapo hapo na kufa. Yoabu na Abishai wakamkimbiza Abneri ili kulipiza kisasi. Na jua likachwa, naye Abneri akakimbia. Mwishowe Abneri akiwa na kabila la Benyamini akazungumza na Yoabu aache kuleta uchungu zaidi kwa mauaji mengine. Yoabu akapiga tarumbeta na watu wakasimama na kuacha kuwafuatilia Abneri ili kupigana nao. Wakahesabu watu wao 19 upande wa Yoabu na 360 upande wa Abneri walikuwa wamelala mauti. Wakamchukua Asaheli ndugu yao, wakasafiri usiku kucha, waende kumzika kwao Hebroni. Kulikuwa na vita siku nyingi kati ya nyumba ya Sauli na Daudi. Daudi akastawi, ila nyumba ya Sauli ikazidi kudhoofika. Daudi akapata wana kule Hebroni, mzaliwa wake wa kwanza aliitwa Amnoni

kwa Ahinoamu, na wa pili Danieli kwa Abigaili, na wa tatu Absalomu na wengine Adoniya, Shefatia, Ithreamu. Ikawa vita kati ya nyumba ya Sauli na Daudi. Abneri alipata nguvu katika nyumba ya Sauli, na akaapa kumsaidia Daudi na kuwa upande wake "Kama BWANA alivyomwapia; kuupitisha ufalme toka nyumba ya Sauli, na kukisimamisha kiti cha Daudi juu ya Israeli." Ishboshethi akaogopa kumjibu Abneri akijua aliweza kusimama na kutawala kwa sababu yake, na akitoka hatakuwa na uwezo wowote.

Nchi za jirani, na raia wengine walijua kuwa Mungu wa mbinguni alikuwa pamoja na Daudi. Mafanikio yanadumu endapo tunatii mapenzi ya Mungu na kutafuta ushauri Kwake kwa kusali na kusoma Neno Lake.

*Wengi sana, katika kupanga maisha mazuri ya baadaye, huishia kushindwa kabisa. Mwachie MUNGU akupangie. Kama mtoto mdogo, tumaini mwongozo Wake Yeye ambaye "atashika miguu ya watakatifu Wake." 1 Samweli 2: 9. Mungu kamwe hawaongozi watoto Wake tofauti na vile ambavyo wangechagua kuongozwa, ikiwa wangeweza kuona mwisho tangu mwanzo na kutambua utukufu wa kusudi ambalo wanalitimiza kama watenda kazi pamoja Naye.


---

Sauli alikufa pamoja na nani? Kwa nini Daudi aliwapa tunu gani watu wa Yabesh-Gileadi? Kwa nini Ishboshethi aliogopa kumjibu Abneri? Kwa nini Yoabu na Abishai walimkimbiza Abneri? Kwa nini kijana Mwamaleki alisema uongo? Ushindani katika michezo, ubinafsi, kuharibu mali, na kujiingiza michezo leo kunaweza kuwa chanzo cha dhambi nyingi, elezea zaidi hili? Ni masomo gani tunaweza kujifunza kutokana na mwisho mbaya wa mtu Mfalme Sauli ambaye alikuwa amejazwa na Roho wa Mungu?

**SIKU YA 88**
**(Machi 28)**

# Daudi Atawala Hebroni na Israeli Yote

**- 2 Samweli 3-5**



Abneri akijua kwamba Daudi anapendwa na watu na ndiye chaguo la BWANA, alituma wajumbe kwa Daudi akisema, "mkono wangu utakuwa pamoja nawe, ili kuwaleta Israeli wote kwako." Daudi akasema vyema kwa sharti la kuletewa mke wake wa kwanza, yaani, Mikali binti wa Sauli, ndipo wataonana uso kwa uso. Basi Daudi alituma ujumbe kwa Ishboshethi kumleta Mikali, aliyemposa na kumtolea mahari. Ishboshethi akaenda kumchukua kwa Paltieli mwana wa Laishi alipoolewa tena, naye mumewe akamfuata akilia mpaka Abneri akamwambia rudi, naye akarudi. Abneri akafanya mashauri na wazee wa Israeli na kusema, jinsi walivyotaka zamani Daudi awamiliki, basi sasa wafanye hayo, kwa maana BWANA "amemtaja Daudi akisema kwa mkono wa mtumishi wangu, Daudi nitawaokoa watu wangu Israeli katika mikono ya Wafilisti, na mikono ya adui zao wote. Abneri akazungumza na Wabenyamini na Waisraeli, kisha wakaenda kwa Daudi kwa karamu, na akapanga kumkusanyia Daudi watu wote ili kufanya agano la kutawala kwa wote wanaompenda.

Daudi kwa roho njema na kusamehe yote Sauli na Abneri waliyomfanyia, aliafikiana na Abneri. Abneri akaenda kwa amani, na Yoabu akaja kutoka jeshini na mateka na kusikia jinsi Abneri alivyozungumza na binamu yake Daudi. Yoabu Akamwambia Daudi, "Abneri ni mdanganyifu apate kujua kutoka kwako, na kuingia kwako, akajue yote utendayo." Yoabu akamfuata Abneri na kumchukua kando kwa faragha, kisha akampiga mkuki wa tumbo mpaka akafa, akilipiza damu ya Asaheli ndugu yake. Daudi alishtuka, maana hakujua hila ya Yoabu na akasema, "mimi na ufalme wangu hatuna hatia milele mbele za BWANA, kwa sababu ya Abneri mwana wa Neri. Na imwangukie Yoabu kichwani pake, na nyumba ya babaye." Kisha Daudi aliwaambia Yoabu na watu wote wararue nguo na kujivika magunia, wamlilie Abneri. Wakaenda kumzika Abneri huko Hebroni, mfalme akilia kaburini nao watu wote wakalia, alisema, "Ilimpasaje Abneri kufa afavyo mpumbavu? Mikono yako haikufungwa, wala miguu yako haikutiwa pingu; Aangukavyo mtu mbele ya wana wa uovu ndiyo ulivyoanguka." Watu wakalia na kumshurutisha Daudi ale, naye akasema hataonja chakula mpaka jua litue. Wote wakafanya kama mfalme, na wakajua kwamba nia ya mfalme ilikuwa njema na hakutaka Abneri auwawe. Daudi akasema, "hamjui ya kuwa mkuu mmoja, naye ni mtu mkubwa, ameanguka leo katika Israeli? Nami leo nimedhoofika, hata nijapotiwa mafuta niwe mfalme, wana wa Seruya ni wagumu kwangu mimi. Bwana amlipe mwovu sawasawa na uovu wake." Seruya alimwoa dada wa Daudi, na hii ilifanya Yoabu na Asaheli kuwa wapwa wa Daudi.

Ishboshethi aliyewekwa kuwa mfalme na Abneri aliposikia kwamba Abneri amekufa, alidhoofika na Waisraeli wote walio upande wake wakataabika na wakakimbia kwenda ugenini. Yonathani alikuwa na mwana aitwaye Mefiboshethi. Huyu akiwa na miaka mitano ndipo walipata habari za kufa kwa Yonathani na Sauli, na yaya wake alimchukua na kukimbia naye kwa haraka naye akaanguka na kupata kilema cha miguu.

Naye Ishbosheti, aliyetawala miaka miwili katika Israeli akauawa na Rekabu na Baana akiwa amepumzika adhuhuri, nao wakijifanya wanachukua ngano, walimpiga mkuki wa tumbo na kukimbia. Nao wakifikiri watamfurahisha Daudi walileta kichwa chake kwake, wakisema, "Tazama, hiki ni kichwa cha Ishoboshethi, mwana wa Sauli adui yako aliyekutafuta roho yako; BWANA amemlipia kisasi bwana wangu mfalme hivi leo." Daudi akaapa kwamba, kama vile yule mtu aliyesema "alimwua Sauli" alivyopata adhabu, ndivyo Rekabu na Baana watakavyoadhibiwa kwani waliua mtu mwenye haki kitandani mwake. Watu hawa wawili waliuawa, na Daudi akamzika Ishboshethi kwenye kaburi la Abneri kule Hebroni. Mambo ya kuwa na mfalme yalileta shida ya mauaji na kupinduana. Wakati wakiwa na waamuzi, ukatili huu haukutokea kwa mwamuzi.

Kabila zote za Israeli walimwendea Daudi huko Hebroni na kusema "sisi tu mfupa wako na nyama yako." Wakamwambia hata Sauli alipokuwa hai, Daudi aliongoza jeshi la Israeli, kuingia na kutoka. Wazee hawa walipatana naye, nao wakamtia mafuta na kumtawaza awe mfalme juu ya Israeli. Daudi alikuwa na miaka 30 alipoanza kutawala. Akatawala miaka arobaini, miaka Saba Hebroni na miaka 33 Yerusalemu. Alitawazwa mara mbili. Akaenda na watu wake kupigana na Wayebusi.

Akautwaa Yebusi, ndio ukawa mji wa Daudi, ngome ya Daudi, ngome ya Sayuni au Yerusalemu. Daudi alisema atakayekuwa wa kwanza kupiga ngome ya Wayebusi ndiye atakuwa jemadari mkuu wa jeshi naye Yoabu mwana wa Seruya akafanya vile. Daudi akazidi kuwa mkuu; kwa maana BWANA Mungu wa majeshi alikuwa pamoja naye.

Hiramu mfalme wa Tiro akatuma wajumbe na kumpelekea Daudi mierezi, maseremala, na waashi; nao wakamjengea Daudi nyumba; Hiramu akawa rafiki yake akijua kwamba BWANA amemweka imara awe mfalme juu ya Israeli, na ufalme Wake umetukuka kwa ajili ya watu Wake Israeli. Wafilisti wakaja kwa Daudi, kufanya vita, naye akamwuliza BWANA kuwa apande juu ya Wafilisti? Naye BWANA akasema, Panda, kwa kuwa hakika nitawatia Wafilisti mikononi mwako. Daudi aliwapiga huko na kusema BWANA amewafurikia adui zangu mbele yangu, kama mafuriko ya maji. Wafilisti waliacha sanamu zao huko na Daudi na watu wake wakaziondolea mbali. Wafilisti walikuja tena, na Alipouliza kwa BWANA akajibiwa "usipande; zunguka nyuma yao, ukawajie huko mbele ya miforosadi." Alifanya vile na kushinda tena.

Daima katikati ya huzuni na kuchanganyikiwa, Daudi alijitia moyo, au alijitia nguvu mwenyewe katika Bwana. Akamwomba Mwenyezi Mungu ushauri afanye nini, Naye Mwenyezi Mungu akamuongoza, na tatizo hilo likatatuliwa. Nasi tujifunze wakati wa shida na huzuni kwa kukumbuka ahadi za Mungu. Tukumbuke kwamba ametuahidi, akisema, "Upitapo katika maji mengi, nitakuwa pamoja nawe; Na mito haitakugharikisha. Upitapo katika moto, hutateketea, Wala mwali wa moto hautakuunguza. Tunapaswa kuepuka kufa moyo kiasi kwamba tusanahau ahadi hii, kwani kuikumbuka na kuidai ni mwanzo wa ufumbuzi wa kutoka kwenye shida, au kuweza kuishi nayo kwa ujasiri.

*Kristo katika maisha Yake humu duniani hakujifanyia au kujipangia mikakati ya ratiba ya maisha Yake Yeye Mwenyewe. Alikubali mipango ya MUNGU Kwake, na siku hadi siku Baba aliifunua mipango Yake. Ndivyo nasi tunavyopaswa kumtegemea MUNGU, ili maisha yetu yaweze kuwa na utekelezaji rahisi yaani mtelemko unaoelekea kwenye mapenzi Yake. Tunapomkabidhi njia zetu, Yeye ataziongoza hatua zetu.

---

Kwa nini Abneri alimwendea Daudi? Kwa nini Paltieli alinyang'anywa mke? Kwa nini Yoabu alimwua Abneri? Nini tunajifunza kuhusu tabia ya Yoabu? Daudi alitawala miaka mingapi? Je, kwa nini wengi hawamwulizi BWANA ushauri tofauti na alivyofanya Daudi? Chunguza kuhusu miforosadi (aina ya berries) ambazo ni za mitini na zinastawi Afrika, haya ni matunda ya afya, yanayotumika kulisha vipepeo wa kutengeneza kitani, kingereza mulberry tree.

**SIKU YA 89**
**(Machi 29)**

# Sanduku la BWANA Larudi

**- 2 Samweli 6-7**



Daudi akaendelea kuwa mkuu, kwa maana BWANA wa majeshi alikuwa pamoja naye. Daudi alikusanya watu 30,000 na kwenda nao ili kulipandisha sanduku la Mungu lililoitwa kwa Jina, naam, Jina la BWANA wa majeshi akaaye juu ya makerubi. Wakaweka sanduku la BWANA juu ya gari jipya, wakalitoa katika nyumba ya Abinadabu, iliyoko kilimani. Sanduku hili lilikaa kule miaka mingi, tokea wakati wa Eli. Uza na Ahio wana wa Abinadabu wakaliendesha lile gari jipya. Ahio alitangulia na Daudi na nyumba yote ya Israeli wakacheza mbele za BWANA kwa nguvu zao zote, kwa nyimbo, vinubi, vinanda, matari na matoazi. Wakafika uga wa Nakoni na Uza ndugu ya Ahio alinyosha mkono akalikamata sanduku, maana ng'ombe walijikwaa. Ndipo hasira ya BWANA ikawaka juu ya Uza, Naye Mungu akampiga huko kwa kosa lake na akafa palepale penye sanduku la Mungu. Watu wengi wameuliza kwa nini Uza aliuawa? Ila maagizo ya kubeba Sanduku la Agano yalikuwa yamewetolewa na kufuatwa kwa zaidi ya miaka 400. Daudi akaona uchungu kwa hasira ya Mungu kwa Uza, na Daudi akamwogopa Mungu siku ile akisema "Litanijiaje sanduku la BWANA?" Daudi hakutaka kulileta sanduku la Bwana mjini kwake, naye akalihamishia nyumbani kwa Obed-edomu, mgiti kwa miezi mitatu, naye Obed-edomu akabarikiwa na nyumba yake yote. Nasi leo tunaweza kubarikiwa kama Obed-edomu endapo tutakubali kuwa wakarimu na

wenye bidii katika mambo ya Mungu.

Daudi aliposikia baraka alizokuwa anapata Obed-edomu, na vitu vyote alivyo navyo kwa ajili ya sanduku la Mungu, alienda akalileta lile sanduku toka huko kuja mjini mwa Daudi kwa shangwe. Daudi akatoa kafara na kufurahi mbele za BWANA kwa nguvu zake zote; na alikuwa amevaa naivera ya kitani. Wakaja kwa shangwe, na sauti ya tarumbeta, hata sanduku lilipoingia mjini mwa Daudi. Mikali, mkewe wa kwanza, alichungulia dirishani na kumwona mfalme akiruka ruka na kucheza mbele za BWANA, "akamdharau moyoni mwake." Waliingiza sanduku hili na kuliweka kwenye hema aliyoijenga Daudi. Daudi akatoa dhabihu za amani na kuteketezwa mbele za BWANA na akawabariki watu kwa Jina la BWANA wa majeshi. Akawagawia kila mtu mkate, nyama, na zabibu, kisha wakaenda makwao naye akarudi kwake. Na Mikali mke wake aliyekuwa binti wa Sauli alitoka kumlaki na kumdhihaki akisema "mfalme wa Israeli alikuwa mtukufu leo namna gani, akijifunua mwili wake mbele ya vijakazi vya watumishi wake, mfano wa watu baradhuli bila aibu." Daudi alimweleza mke wake jinsi moyo wake ulivyo na shukurani na furaha, kwamba katika shida zake zote za miaka mingi, na hata vita na mateso, "BWANA aliyenichagua mimi juu ya baba yako, na juu ya nyumba yake, ili kuniweka mkuu juu ya watu wa BWANA, juu ya Israeli; kwa hiyo mimi nitacheza mbele za BWANA. Kisha nitakuwa hafifu zaidi, nami nitakuwa mnyonge machoni pangu mimi mwenyewe" ila wafanyakazi unaosema watanidharau, kwao nitaheshimiwa. Basi Mikali kwa tendo hili la kudharau kujinyenyekeza na kumfurahia BWANA na mume wake baada ya BWANA kumtendea mema, "hakuwa na mtoto hata siku ya kufa kwake." Hili ni fundisho kwa wale wanaomng'ong'a au kumbeza mtu wakififikiri anajiaibisha akimsifu BWANA au kutoa ushuhuda mbele za watu. Kamwe tusifikiri kwamba tunaonekana wa hadhi ya juu tusipotoa ushuhuda mbele ya watu! Daudi anasema mara nyingi, nitakusifu mbele za watu! Kumsifu au kumshukuru ukiwa peke yako ni muhimu, ila pia mbele za watu ni muhimu! Maana Biblia inasema wakamshinda Shetani kwa damu ya Mwanakondoo na Neno la mdomoni mwao- Ufunuo 12:11.

Ikawa mfalme alipostarehe bila kuudhiwa na maadui, akamwambia Nathani nabii "mimi ninakaa katika nyumba ya mierezi, bali sanduku la Mungu linakaa ndani ya mapazia." Akaielezea nia yake ya kutaka kujenga hekalu, naye Nabii Nathani hakuona cha kuzuia kujenga hekalu, hivyo akamjibu, "fanya yote yaliyomo moyoni mwako; maana BWANA yu pamoja nawe." Lakini usiku huo, BWANA akazungumza na Nathani akisema, "Ukamwambie mtumishi Wangu Daudi, BWANA asema hivi. Je! Wewe utanijengea nyumba Nikae ndani yake? Kwa maana Mimi sikukaa ndani ya nyumba tangu siku ile niliyowatoa wana wa Israeli katika Misri hata leo, lakini nimekaa katika hema na maskani." Mungu akasema hajawahi kusema na waamuzi wa Israeli au yeyote kumjengea nyumba. Naye akasema kuwa alimtwaa katika zizi la kondoo, katika kuwaandama kondoo, ili awe mkuu juu ya watu Wake Israeli. "Nami nimekuwa pamoja nawe kila ulikokwenda, na kuwakatilia mbali maadui zako wote mbele yako, Nami nitakufanyia jina kuu, kama wakuu walioko duniani…Nami nitakustarehesha mbele ya adui zako wote." Akasema kwamba atafanya ufalme unaomfuatia kuwa imara na mzao wake atakayetoka nyuma yake ndiye "atakayejenga nyumba kwa jina Langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake

nitakifanya imara milele. Mimi nitakuwa Baba yake, naye atakuwa mwanangu; akitenda maovu nitamwadhibu kwa fimbo ya binadamu na kwa mapigo ya wanadamu. Lakini fadhili Zangu hazitamwondoka, kama vile nilivyomwondolea Sauli … nyumba yako, na ufalme wako vitathibitishwa milele mbele zako. Nacho kiti chako kitafanywa kuwa imara milele." Hebu nasi leo tuamini kwa Mungu ni Baba yetu, sisi tu wana Wake! Changamka kwa hilo!

Daudi akashukuru kwa ujumbe, akaketi mbele za BWANA na kusema, "Mimi ni nani, BWANA Mungu, na nyumba yangu ni nini hata umenileta hata hapa? … hata umeleta habari ya nyumba yangu … miaka mingi inayokuja baadaye … na mimi Daudi nikuambie nini tena zaidi? … tena ni taifa lipi duniani lililo kama watu wako, kama Israeli… Jina Lake litukuzwe milele." Basi ndivyo Daudi alivyomsifu BWANA kwa Zaburi, nyimbo na tenzi. Akaona kwamba, "Kuwa nyuani mwa BWANA siku moja ni bora kuliko siku 1000 mahali pengine." Daudi akaelewa, kwa sababu alikuwa amemwaga damu na kuwa mtu wa vita miaka mingi, yeye hatamjengea BWANA hekalu bali mtoto wake Sulemani aliyeishi wakati wa amani atafanya vile. Daudi akaanza kukusanya vifaa vya ujenzi na kuchora michoro ya jengo.

Mungu alitunza agano na Daudi na nyumba yake ilibarikiwa milele kupitia kwa masihi. Yesu Ndiye aliyefanya ufalme wa Daudi uwe imara. Ni uzuri ulioje kukaa na kuzungumza na BWANA kama Daudi? Hata sisi tunaweza kukaa na kuzungumza na BWANA maneno au mazungumzo matamu, kama Daudi, Naye atazisimamisha nyumba zetu milele. Tukumbuke kuwa ahadi aliyompatia Daudi miaka ile, ni yetu pia!

Si lazima tujenge hekalu tukufu kama mahali pa kuabudu, lakini ni lazima tuandae mioyo yetu kwa ajili ya ibada. Je, unajiandaaje? Daudi, baba ya Sulemani, alisema hivi: "Ni nani awezaye kupanda katika mlima wa BWANA? Au ni nani awezaye kusimama katika patakatifu pake? Yeye aliye na mikono safi na moyo safi, asiyeinua nafsi yake kwa sanamu, wala hakuapa kwa hila" (Zaburi 24:3-4). Tunajua hali ya kiroho ya ulimwengu leo, na kile ambacho Mungu ametutuma kukifanya. Tumeweka mikono yetu kwenye mpini wa jembe ili kufanya kazi ya Mungu. Tunakabili upinzani wa kila namna, lakini hatupaswi kutazama nyuma, kuzuiwa au kukengeushwa. Mungu yu pamoja nasi. Atatufanya tufanikiwe katika kazi tunayofanya, kwa maana ni kazi yake tunayoifanya. Sauli na maadui wengine wa wakati wetu hawana sehemu au haki katika jukumu tulilopewa. Kwa hiyo, tundelee, maaskari Wa Kristo!

*Ikiwa umejitoa kwa MUNGU kuifanya kazi Yake, hauna haja ya kuwa na wasiwasi juu ya kesho. Yeye ambaye wewe ni mtumishi Wake, anajua mwisho tangu mwanzo. Matukio ya kesho, ambayo yamefichwa machoni pako, yako wazi machoni Pake Yeye aliye na nguvu zote.

---

Sanduku la agano lilikaa kwa watu wawili, ni akina nani hao? Kwa nini Uza aliuawa? Kwa nini Mikali hakupata mtoto? Kwa nini Daudi aliambiwa na BWANA mtoto wake ndiye atajenga hekalu? Nasi leo tunawezaje kuzungumza na BWANA?

**SIKU YA 90**
**(Machi 30)**

# Kurudisha Hisani Kupitia kwa Mefiboshethi

**- 2 Samweli 8-10**

Daudi aliendelea kukomboa nchi mbalimbali. Akaipiga Gathi na Moabu, nao wakawa watumwa wake na kumletea zawadi. Akapokonya wapanda farasi 1700 wa mfalme wa Soba na askari 20,000. Daudi akawapiga Washami wa Damesiki, na kuweka ngome Dameski, na kuteka nyara za dhahabu na shaba na kuviweka wakfu kwa Bwana. Akawashinda, Waedomu, Wafilisti, Waamoni, Waamaleki na wengineo. Naye BWANA akampa Daudi kushinda kila alikoenda, nasi pia anaweza kutusaidia kufanikiwa, na kuishi maisha ya kumcha Yeye tukishinda dhambi kila tunakoenda. Je! Si jambo la kutupatia tabasamu hilo? Basi akatawala Israeli na kufanya hukumu kwa watu Wake, naye Yoabu alikuwa amiri Jeshi wake, Ahiludi mwenye kutunza rekodi, Sadoki na Ahimeleki makuhani wake, Benaya balozi wake. Wanawe wa kiume wakawa washauri katika ufalme wake.

Naye Daudi alitaka kujua kama amesalia mtu yeyote katika nyumba ya Sauli ili aweze kurudisha hisani, kwa ajili ya Yonathani rafiki yake. Siba alikuwa mtumishi wa Sauli, na akaitwa kwa Daudi, na mfalme akauliza kama kuna mtu wa nyumba ya Sauli "nipate kumtendea mema ya Mungu." Siba akasema, Yonathani ana mwana mwenye kilema cha miguu miwili, naye Daudi akauliza, alipo. Basi Mefiboshethi, mwana wa Yonathani, aliyekuwa kwa Makiri akaletwa, na alipofika kwa Daudi, alianguka kifudifudi na kusujudu. Daudi akamtuliza na kumwambia "Usiogope, maana bila shaka nitakutendea mema kwa ajili ya Yonathani, baba yako." Akamrudishia mashamba yote ya Sauli, na akamwalika akae naye ikulu, na kula chakula cha mezani kwake daima. Naye Mefiboshethi kwa unyenyekevu, akijua ni hisani, kubwa, hasa akijua hila za babu yake Sauli alijibu "Mimi mtumwa wako ni nani, hata ukamwangalia mbwa mfu kama mimi?" Mfalme akamwita Siba na kumpa ile mali amsaidie mtoto wa Sauli kuitunza, na kulima mashamba na kuvuna. Naye Siba akakubali, na Mefiboshethi alikaa kula chakula cha mfalme, siku zote kama mmojawapo wa mwana wa wafalme, naye alikuwa ana mtoto aliyeitwa Mika. Jambo jema kiasi gani, kutosahau fadhili kwa wale wanaotufanyia mema? Nafikiri Mefiboshethi alifurahi, kwani hata wewe ungekaa ikulu, na mfalme ni rafiki wa baba, ungejisikia kidogo!

Mfalme wa Amori aliyekuwa na mahusiano mazuri na Daudi akafa, na mtoto wake Hanuni akarithi ufalme. Daudi alikuwa na moyo wa kirafiki, ila watu wengine ukiwaonesha mema, hulipa uovu. Hili ni vyema kulijua ili usivunjwe moyo. Basi Daudi aliamua kupeleka ujumbe wa kumtuliza kwa kifo cha babaye. Watumishi wake walipokuja huko Amoni, Hanuni na watu wake wakasema, wajumbe hao ni wapelelezi, na wanataka kuangamiza mji. Hanuni aliwatwaa watumishi wa Daudi na kuwanyoa nusu ya ndevu zao, na kuwakatia nguo zao, kisha akawaambia "nendeni kwenu." Watu walipotuma ujumbe kwa Daudi kuhusu

yaliyotokea, alituma ujumbe kwa watu hawa waliokuwa wametahayari, akiwaambia wangojee Yeriko mpaka watakapoota ndevu zao ndipo warudi. Waamoni wakajua wamemchokoza Daudi na wakajihami kwa kuajiri majeshi ya kukodiwa ya Washami na wengine. Daudi akamtuma Yoabu na jeshi lake la mashujaa, naye akaona jeshi la kukodiwa limejaa kwake nyuma na mbele, na Washami walikuwa hodari mno. Akapanga na ndugu yake Abishai jinsi ya kusaidiana, "wakiwa Washami hodari mno kwangu, ndipo wewe utanisaidia, wana wa Amoni wakiwa ni hodari mno kwako, mimi nitakuja nikusaidie wewe ,.. tukajitie moyo mkuu, kwa ajili ya watu wetu, na kwa ajili ya miji ya Mungu wetu." Washami wakakimbia, na Waamoni walipoona mashujaa waliowakodi wamekimbia, nao pia wakakimbia. Kisha wafalme hawa walipoona kwamba wameshindwa walijisalimisha kwa Israeli kwa kufanya amani na kuwatumikia. Basi Washami wakaogopa kuwasaidia wana wa Amoni tena. Upumbavu wa namna gani, wa kutenda ujeuri kwa watu, na kisha tuwatumikie, badala ya kuwa na hekima na kujenga urafiki ili nasi tuwe watu huru ni kujiangamiza. Dhambi inatufanya tumtumikie Shetani na binadamu siku zote.

Hakuna nguvu inayoweza kuyaangamiza mapenzi ya Mungu, Yeye ni Mweza yote, hakuna nguvu inayoweza kuyaangamiza. Hakuna mtu anayeweza kuharibu kile Mungu amekipanga kwaajili ya yeyote wa watoto Wake. Daudi alikuja kuchukua ule wadhifa Mungu aliompangia, na kuonyesha wema kwa jamaa ya Sauli. Lakini inabidi kungoja wakati uliowekwa ili mipango Yake itimie. Daudi alilazimika kungoja kwa miaka saba na nusu, baada ya kifo cha Sauli, ili awe mfalme wa Israeli. Mungu Ndiye anayeadhibu makosa yanayofanywa kwa Watoto wake kwa maana anasema, "Wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu; kwa maana imeandikwa, Kisasi ni changu Mimi; Mimi nitalipa, asema Bwana. Warumi 12:19 . Letu ni kuwapenda na kuwaombea maadui zetu na uzao wao. Kuwapenda haimaanishi kuwa na hisia changamfu kuelekea maovu wanayofanya, bali kuchagua kuwatendea mema licha ya hisia zisizopendeza tulizo nazo kuhusu wao. Upendo ambao Biblia inautetea hapa ni kanuni, na si hisia. Tuombe uwezo wa kuwapenda adui zetu bila masharti ili "tupate kuwa wana wa Baba yetu aliye mbinguni; kwani Yeye huliangazia jua Lake juu ya waovu na wema, na huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki." Mathayo 5:45.

*Tunapojichukulia mikononi yetu usimamizi wa vitu ambavyo tunapaswa kufanya, na kutegemea hekima yetu wenyewe kwa ajili ya mafanikio, tunajitwika mzigo ambao MUNGU hajatupatia, na tunajaribu kuubeba bila msaada Wake. Tunachukua jukumu ambalo ni la MUNGU, na kwa hivyo tunajiweka wenyewe katika nafasi Yake (GOD's syndrome). Tunaweza kujiletea na wasiwasi na kutarajia hatari na hasara, kutupata kwa hakika. Lakini wakati tunaamini kabisa kwamba MUNGU anatupenda na ana kusudi la kututendea mema tutakoma kuwa na wasiwasi juu ya siku zijazo. Tutamtumaini MUNGU kama vile mtoto anavyomwamini mzazi wake mwenye upendo. Ndipo shida zetu na mateso yatatoweka, kwani mapenzi yetu yamemezwa katika mapenzi ya MUNGU.

---

Je, BWANA anawezaje kutupatia ushindi kila tunakoenda kama alivyofanya kwa Daudi? Daudi alirudishaje fadhili kwa Yonathani? Hunani alisababishaje ugomvi?

Mefiboshethi alipataje kilema cha miguu? Chunguza maisha yako jinsi ambavyo dhambi inakufanya uwe mtumwa.

**SIKU YA 91**
**(Machi 31)**

# Dhambi Kubwa ya Daudi

**- 2 Samweli 11**



Daudi aliacha kwenda vitani, ila akamtuma Yoabu. Wakapigana na Waamoni wakashinda. Mpaka hapa, Daudi alijulikana kwa mambo mema, hadi alipokaa Yerusalemu, na akabarizi, hata kupata muda wa kulala usingizi wa mchana na kutembea darini kwenye jumba la kifalme. Alipendwa na watu na Mungu, akiwashindia vita na kuwasaidia kuhukumu kwa haki. Mungu alimpandisha akatawala toka Misri mpaka mto Frati.

Kutokuwa na shughuli ya kufanya, au ubongo usio na shughuli, ni karakana ya Shetani kutushughulisha na mitego yake. Nyumba yake ilikuwa na dari juu, na hivyo kuweza kuona raia wake walio chini. Siku moja alipokuwa akitembea juu ya dari akiangalia himaya yake, aliona mwanamke aliyekuwa mzuri sana anaoga. Inaonekana siku zile watu walikuwa na mabafu kama ya kwetu vijijini, yasiyo na paa, na hivyo kama mtu aliyeko ghorofani anakuona. Daudi akapata tamaa, na akapeleleza kujua habari za yule mwanamke. Akaambiwa jina lake ni Bath-sheba, na ni mke wa mtu aitwaye Uria Mhiti, mwanajeshi wake mwaminifu. Uria alikuwa mhiti aliyeongoka na kumfuata Mungu wa Israeli; hakuwa Mwisraeli, bali alimfuata Mungu wa Israeli. Daudi akapeleka wajumbe kumtwaa huyu mwanamke na kulala naye kama mke wake. Kisha yule mwanamke alirudi nyumbani mwake. Hapa tunajifunza kulinda njia za moyo, yaani kile macho yetu kinatazama, kile masikio kinachosikia, kile mikono yetu inachogusa, kile tunachonusa, na pale tunapopeleka miguu yetu. Ibada ya asubuhi na jioni waliyofanya Waisraeli ilipaswa kusaidia kulinda moyo, kwani sote tusiporudi kwenye ibada binafsi asubuhi na jioni, na kufikiria ya Bwana siku nzima tutajiingiza mitegoni.

Baada ya muda, yule mwanamke aligundua kuwa ana mimba ya Daudi na akatuma ujumbe kwa Daudi kwamba ni mjamzito. Hapo ndipo Daudi alitaka mimba hiyo ionekane ya mume wake na si yake. Akamtuma Yoabu amtoe Uria jeshini akae nyumbani, ili ile mimba ijulikane kwamba ni ya Uria, na si yake mfalme. Akamwambia binamu yake, “unipelekee Uria, Mhiti.” Yoabu akamleta Uria, naye Daudi akamwuliza habari za bosi wake Yoabu na vita; kisha akamwambia aende nyumbani kwake. Uria akatoka amekula tunu ya vyakula vya mfalme, ila akalala mlangoni pa nyumba ya mfalme pamoja na watumishi na jeshi la Israeli, wala

hakushuka nyumbani kwake. Watu wakamwambia Daudi, Uria hakwenda kwake japo alipata ruhusa. Mfalme, akamwuliza kwa nini hakwenda nyumbani, naye ametoka safari na mfalme amempa ruhusa. Ndipo Uria, Mhiti alijibu kwa uaminifu na kuwajibika akisema, sanduku na Israeli…na Yoabu … na watumishi wamepiga kambi, wako nje uwandani, nami niende kula na kunywa na kulala na mke wangu? Kama aishivyo mfalme, mimi sitafanya jambo hilo. Mfalme akamweka Uria siku mbili, na akamwalika na kumpa pombe ili alewe, na kwenda kulala nyumbani kwake, lakini hakwenda kwake. Ndipo asubuhi ile Daudi aliandika barua, akampelekea Yoabu ili amweke Uria kwenye mstari wa mbele wa mapambano ya vita vikali, "kisha ondokeni mmwache, ili apigwe akafe." Akaenda akihusuru mji wa mashujaa, na walipotoka ili wapigane akamweka Uria mstari wa mbele na akafa na watumishi wengine wa Daudi.

Yoabu akapeleka habari kwa mfalme. Ndipo aseme "mtumishi wako Uria, Mhiti amekufa naye." Basi haya yote yalifanyika na Daudi akitaka kuendeleza ule uongo, baada ya kuzini, kumpa mtu kileo, kusema uongo na kuua, alisema "jambo hili lisiwe baya machoni pako, maana upanga hula huyu kama unavyomla huyu, zidi kutia nguvu vita …" Mjane Bath-sheba alipomaliza maombolezo ya mumewe Uria, Daudi alituma mtu na kumchukua awe mke wake. Daudi akafanya kama mfalme wa mataifa yasiyomjua Mungu. Ni rahisi kuota pembe za kiburi tukifanikiwa na kuwa na mali, na kujisahau kwamba tulikuwa maskini, na Mungu ametutoa kwenye matope. Daudi alimpenda Mungu kwa dhati,hata kuambiwa 'mtu anayeupendeza moyo wangu.' Biblia ikisimulia inasema mabaya na mazuri ya mtu, si kama sisi tukiandika habari za ndugu zetu tunazipamba sana. Habari hii ya Daudi imeandikwa ili kuwa fundisho kwetu, kwamba Mungu ni mwenye huruma, bali kuna adhabu na tunapotubu na kuacha njia mbaya, anaturudi na kufuta maovu yetu yote. Mfalme akafikiri limepita, "lakini jambo lile alilolitenda Daudi likamchukiza BWANA."

Wanaume wanaoongoza katika historia ya Biblia wamefanya dhambi nzito. Dhambi zao hazifichwi, bali zimeandikwa kwa uaminifu katika historia ya kanisa la Mungu, pamoja na adhabu kutoka kwa Mungu, iliyofuatia makosa. Matukio haya yameachwa kwenye kumbukumbu kwa manufaa ya vizazi vinavyokuja, na yanapaswa kutupa imani katika Neno la Mungu, kama historia ya kweli, aminifu na halisi. Mungu hapambi-pambi dhambi za watu pale wanapofanya wanapokosea, haijalishi wao ni nani, husema mambo kama yalivyo, kwa faida ya mtenda dhambi na wasomaji ili tuichukie dhambi na tutubu. Watu hawa walijaribiwa na Shetani, na madhaifu na dhambi zao hazijafunikwa, bali zimeandikwa kwa uaminifu, pamoja na makaripio na adhabu zilizofuata. Mambo hayo "yaliandikwa ili kutuonya sisi tuliofikiliwa na miisho ya dunia."

Mungu hajaruhusu mengi yasemwe katika Neno lake katika kusifia wema wa watu bora zaidi ambao wameishi duniani. Ushindi wao wote, na matendo makuu na mema, yalihesabiwa kwa Mwenyezi Mungu. Yeye peke Yake Ndiye alipaswa kupokea utukufu, Yeye peke Yake tu, Ndiye ambaye angeinuliwa. Alikuwa yote na katika yote. Mwanadamu alikuwa wakala tu, chombo dhaifu mikononi Mwake. Nguvu na ubora wote vilikuwa vya Mungu. Mungu aliona ndani ya mwanadamu tabia

ya kuendelea kumwacha, na kumsahau, na kuabudu kiumbe badala ya Muumba. Kwa hiyo, Mungu hakuacha sifa za mwanadamu zijae kwenye kurasa za historia takatifu bila maelezo yale ambayo ni ya kweli kabisa.

*Eliezeri Aliomba kwa ajili ya—na Akapokea—Mwongozo wa MUNGU—Akikumbuka maneno ya Abrahamu, kwamba MUNGU atamtuma malaika Wake pamoja naye, alisali kwa dhati na bidii ili kupata mwongozo chanya. Katika familia ya bwana wake alikuwa amezoea mazoezi ya mara kwa mara ya fadhili na ukarimu, na sasa aliomba kwamba kitendo cha ukarimu wa mwenyeji wake kiweze kuonyesha na msichana ambaye MUNGU alimchagua.

---

Kwa nini Yoabu jemedari alikubali kumsaidia binamu yake kumwua Uria? Kwa nini Bath-sheba hakukataa kwenda kwa mfalme? Kwa nini Uria hakukubali aende nyumbani mwake? Orodhesha amri alizovunja Daudi. Kwa nini kumpa mtu kileo ni dhambi? Kwanini Biblia inataja kila kitu wazi, yaani hata zile dhambi za wapendwa na wakuu? Tujipeleleze uovu ulioufícha, na tuwe wakweli. Kwanini Biblia ndiyo biografia pekee ambayo ina kweli yote?

**SIKU YA 92**
**(Aprili 1)**

# Adhabu ya Daudi

**- 2 Samweli 12**



Unaweza kufikiri, Daudi alikuwa na kila kitu. Biblia inasema 'utauwa na kuridhika ni faida kubwa', kwani tulikuja duniani bila kitu na tutaondoka bila kitu. Mara nyingi tukiwa maskini tunafikiri kwamba hatutafanya kama matajiri. Mtu anaweza kuwa maskini lakini akawa na tamaa zaidi hata ya tajiri, ila nafasi haijatokea kufanya matakwa yake. Tukumbuke kuwa, wale ambao Mungu amewakabidhi mengi, basi watatakiwa mengi. Daudi alikuwa si mfalme tu, bali nabii wa Mungu na mtumishi Wake; "aliwapa adui za BWANA nafasi kubwa ya kukufuru". Zaburi ina unabii mwingi wa Masihi. Daudi alikuwa amezungumza kuhusu Amri za Mungu kwenye Zaburi 119 kwa undani, na sasa alikuwa amezivunja zote! Hakuna anayependa kusimulia habari hii, ila ni lazima isimuliwe, ili kuwa fundisho kwetu. Kwani alikuwa ameleta giza katika Israeli na katika nyumba yake.

Ndipo BWANA akamtuma Nathani nabii amwendee Daudi na kumwambia kisa cha watu wawili kwenye mji mmoja. Mmoja alikuwa tajiri, na wa pili maskini, yule tajiri alikuwa na ng'ombe na kondoo wengi sana, bali maskini hakuwa na kitu ila

mwana-kondoo mmoja mdogo aliyemnunua na kumlea, akakua pamoja naye kama mwanawe; na kula posho yake, akikinywea kikombe chake na kulala kifuani mwake, akawa kama binti. Naona watoto wengi wa nchi za magharibi wakilala na wanyama wao wa kufugwa kama paka, mbwa, au kondoo, wakionesha upendo kwa wanyama hawa kama huyu mtu. Nathani nabii akaendelea kusema, mtu yule tajiri siku moja alipata mgeni, naye akaacha kumtwaa kondoo wake amchinjie mgeni, bali aliendа kwa maskini na kumnyang'anya kondoo wake na kumchinja ili amwandalie yule msafiri aliyemfikilia. Alipomaliza tu kueleza kisa, Daudi ambaye alijulikana kama mtu wa haki, alihamaki kwa hasira sana juu ya tajiri na kusema "Aishivyo BWANA, mtu huyo aliyetenda jambo hili, hakika yake astahili kufa; naye atamrudishia yule mwana-kondoo mara nne kwa sababu hakuwa na huruma." Ndipo Nathani kwa ujasiri, alisonda kosa lake, akisema, "wewe ndiwe mtu huyo."

Akamwambia BWANA Mungu wa Israeli alimweka kuwa mfalme na kumwokoa na Sauli, na kukupa nyumba na wake, na Yuda na Israeli, kama hayo yangalikuwa machache, angalimwongeza mambo kadha wa kadha au angeomba. Akamwambia amelidharau Neno la Bwana na kufanya mabaya mno machoni Pake. "Umempiga Uria, Mhiti kwa upanga, nawe umemtwaa mkewe awe mke wako, nawe umemwua huyo. Basi sasa upanga hautaondoka nyumbani mwako kwa sababu umenidharau. Bwana akamwambia kwamba atamwondokeshea uovu nyumbani mwake na watu watatwaa wake zake mbele ya macho yake na kulala nao; "maana wewe ulifanya jambo lile kwa siri; bali Mimi nitalifanya jambo hili mbele ya Israeli wote na mbele ya jua." Daudi akaomba akajuta na kuomba msamaha, na akaona kweli dhambi yake iko mbele za Mungu, akakiri akisema, "Nimemfanyia Bwana dhambi." Nathani alipoona majuto yake, yaani, mfalme hakubisha, bali aliungama, alimwambia, "BWANA Naye ameiondoa dhambi yako; hutakufa." Kama angebisha asiiungame angeliuawa. Nathani akaondoka kwenda nyumbani kwake na Daudi akalia akifunga toka asubuhi akilala kwenye sakafu, maana aliambiwa mtoto atakayezaliwa na Bath-sheba atakufa. Wazee wa ikulu wakakaa karibu naye wamwinue afarijike, naye hakukubali, wala hakula pamoja nao.

Siku ya saba mtoto akafa, watumishi wakaogopa kumwambia wakisema alivyomlilia mtoto akiwa mgonjwa atazidi kujisumbua zaidi. Akaona wananong'onezana, wanamficha, na akatambua kwamba mtoto amekufa. Akaamka na akaoga, akajipaka mafuta, na kubadili nguo kisha akaingia nyumbani mwa BWANA akasali. Walipompa chakula akala, nao wakashangaa, naye akawaambia, mtoto alipokuwa hai nalifunga nikalia, kwamba BWANA atanihurumia, mtoto apate kuishi, lakini sasa amekufa, nifungie nini? Naweza kumrudisha tena? Mimi nitakwenda kwake lakini yeye hatanirudia mimi. Daudi akamfariji mke wake Bath-sheba pia. Baada ya mtoto kufa walizaa mtoto mwingine wakamwita Sulemani. Huyu ndiye alirithi ufalme Naye BWANA akampenda Sulemani. Daudi akampeleka mikononi mwa nabii Nathani ampakate, naye akamwita Yedidia maana yake anayependwa na BWANA. Mungu anataka tuungame, moyo uliopondeka Yeye hataudharau.
"Uumbe ndani yangu moyo safi." Hii inaanza sawasawa, katika msingi kabisa wa tabia ya Kikristo; maana zitokazo moyo zitokako chemchemi za uzima. Ikiwa wote, wahudumu na watu, wangehakikisha kwamba mioyo yao iko sawa na Mungu, tungepaswa kuona matokeo makubwa zaidi kutokana na kazi inayofanywa. Kadiri

kazi yako ilivyo muhimu na inayowajibika, ndivyo ulazima wa kuwa na mioyo safi unavyoongezeka. Neema inayohitajika hutolewa, na nguvu za Roho Mtakatifu zitafanya kazi kwa kila juhudi utakazofanya katika mwelekeo huu.

Ikiwa kila mtoto wa Mungu angemtafuta kwa bidii na kwa ustahimilivu, kungekuwa na ukuaji mkubwa zaidi katika neema. Mifarakano ingekoma; waumini wangekuwa na moyo mmoja na nia moja; na usafi na upendo ungetawala katika makanisa yetu. Kwa kumtazama tunabadilishwa. Kadiri tunavyotafakari zaidi tabia ya Kristo, ndivyo tutakavyofanana zaidi na sura Yake. Njoo kwa Yesu jinsi ulivyo, Naye atakupokea, na kuweka wimbo mpya kinywani mwetu, hata sifa kwa Mungu.

"Usinitenge na uso wako; wala usiniondolee Roho wako Mtakatifu" (Zaburi 51:11). Toba pamoja na msamaha ni zawadi ya Mungu kupitia Kristo. Ni kupitia ushawishi wa Roho Mtakatifu kwamba tunasadikishwa kuhusu dhambi, na kuhisi hitaji letu la msamaha. Hakuna anayesamehewa ila wanaotubu, ila, ni neema ya Bwana ndiyo ifanyayo moyo kutubu. Yeye anafahamu udhaifu wetu, Naye atatusaidia. Tunahitaji kufungua mioyo yetu kwa ushawishi wa Roho, na kupata uzoefu wa nguvu Zake za kubadilisha mioyo yetu. Sababu ya kutopokea msaada zaidi wa kuokoa kutoka kwa Mungu ni kwa sababu njia ya mawasiliano kati ya Mbingu na nafsi zenu imezibwa na udunia, upendo wa kujionyesha, na hamu ya kutaka makuu. Ingawa wengine wanapatanana na desturi na kanuni za ulimwengu, sisi tunapaswa kuumba maisha yetu kulingana na kielelezo cha Bwana. Na Mungu wetu anayeshika maagano ataturudishia shangwe ya wokovu Wake, na kututegemeza kwa Roho Wake.

*Punde baada ya kutolewa maombi na jibu lipatikana papo hapo. Miongoni mwa wanawake ambao walikuwa wamekusanyika kwenye kisima, adabu ya mmoja wao ikawa imemvutia. Yule msichana alipokuwa akitoka kisimani, yule mgeni alikwenda kumlaki, akiomba maji kwenye mtungi ulio begani mwake. Ombi hilo lilipokelewa kwa jibu zuri, na ofa ya kuteka maji kwa ajili ya ngamia pia ikatamkwa na msichana huyu, huduma ambayo ilikuwa ni desturi kwa wageni hata kwa binti za wakuu kufanya kwa ajili ya mifugo na makundi ya baba zao. Kwa hivyo ishara iliyotarajiwa ilitolewa/ilionyeshwa na (Rebeka).

Toba ya Daudi inaweza kusomwa katika Zaburi 32 na 51

---

Kwa nini kisa cha uovu wa Daudi kimeandikwa? Elezea jinsi tajiri alivyofanya na kondoo wa maskini? Kwa nini Daudi alikula aliposikia mtoto amekufa? Yedidia ina maana gani? Kwa nini adhabu ya Daudi ilikuwa kubwa kuliko watu wa kawaida? Je, unakumbuka kuungama kila siku?

**SIKU YA 93**
**(Aprili 2)**

# Toba ya Daudi

**- Zaburi 32 na 51**



Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. Daudi alitubu na kuungama dhambi yake, na kuandika Zaburi. Kutubu na kuungama ni jambo la muhimu mno. Tunaandika angalau machache katika yale aliyosema. Mungu Anasema, "Haya, njoni, tusemezane, dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji." Wale walioona Mlima Kilimanjaro, wanajua jinsi theluji ilivyo nyeupe. Mungu Anasema kama vile mashariki ilivyo mbali na magharibi ndivyo nitaweka dhambi zenu. Ukizidi kwenda magharibi utaona kwamba hazikutani na mashariki. Mungu Anasamehe dhambi zetu tukiwa na toba ya kweli. Nabii Nathani alipomweleza Daudi uovu wake, aligundua jinsi alivyokuwa na uovu mwingi na akaandika kwa machozi akisema, "Ee Mungu unirehemu, sawasawa na fadhili Zako. Kiasi cha wingi wa rehema Zako. Uyafute makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, Unitakase na dhambi zangu. Maana nimejua mimi makosa yangu. Na dhambi yangu ipo mbele yangu daima. Nimekutenda dhambi Wewe peke Yako. Na kufanya maovu mbele ya macho Yako. Wewe ujulikane kuwa Una haki Unenapo, na kuwa safi Utoapo hukumu… Unisafishe kwa hisopo nami nitakuwa safi. Unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe, mifupa

Uliyoiponda ifurahi… Uzifute hatia zangu zote. Ee Mungu Uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu. Usinitenge na uso Wako, wala Roho Wako Mtakatifu usiniondelee, Unirudishie furaha ya wokovu Wako; Unitegemeze kwa roho ya wepesi. Nitawafundisha wakosaji njia Zako, na wenye dhambi watarejea Kwako. Ee MUNGU, Mungu wa wokovu wangu…ulimi wangu utaiimba haki Yako…kinywa changu kitazinena sifa Zako. Maana Hupendezwi na dhabihu, au ningeitoa, Wewe huridhii sadaka ya kuteketezwa. Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu Hutaudharau."

"Heri aliyesamehewa dhambi, na kusitiriwa makosa yake. Heri Bwana asiyemhesabia upotovu, ambaye rohoni mwake hamna hila. Niliponyamaza mifupa yangu ilichakaa, kwa kuugua kwangu mchana kutwa. Kwa maana mchana na usiku mkono Wako ulinilemea. Jasho langu likakauka hata nikawa kama nchi kavu wakati wa kaskazi. Nalikujulisha dhambi yangu, wala Sikukuficha upotovu wangu. Nalisema nitayakiri maasi yangu kwa BWANA, Nawe ukanisamehe upotovu wa dhambi yangu. Kwa hiyo kila mtu mtauwa akuombe wakati unapopatikana. Hakika maji makuu yafurikapo hayatamfikia yeye. Ndiwe sitara yangu, Utanihifadhi na mateso, Utanizungusha nyimbo za wokovu. Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea. Nitakushauri, jicho Langu litakutazama ... Naye mtu mwovu ana mapigo mengi, Bali amtumainiye Bwana fadhili zitamzunguka. Mfurahieni BWANA; shangilieni enyi wenye haki, pigeni vigelegele vya furaha. Ninyi nyote mlio wanyofu wa moyo."

Toba iwe ni lengo letu mara tu tunapogundua kuwa tumefanya dhambi. Mpendwa mtoto, hakuna kilicho mafichoni, kila kitu Mungu anajua, hata tukiwa tumefanya kwa siri, peke yetu, hakuna siri kwa Mungu hivyo ni vizuri kumwambia Yeye na tuiungame. Kisha tunapokuwa tumetubu na kuungama, imetupasa kuamini kuwa tumesamehewa na yote ya kale yamepita, na tuombe nguvu ya kushinda hiyo dhambi, na mara zingine dhambi tulizojiingiza huchukua muda kidogo kutokomea kabisa, ila Mungu ni Mwaminifu, hivyo zitatokomea. Shetani anataka tukate tamaa, tusione mlango wa kutokea tunapofanya dhambi. Usiache hili litokee, sema, Mungu ni mwaminifu Naye ameahidi kunisamehe. Kisha ujifunze kusamehe wengine wakikukosea pia, maana Mungu hutusamehe pale tunaposamehe wengine, na kutokuwa na kinyongo. Hakuna dhambi Mungu asiyosamehe, ila ile ambayo haikuungamwa tu, au kujutiwa. Na tukiungama tuungame kwa kusema dhambi maalum tuliyofanya, tusiseme nimefanya dhambi tu kwa jumla, ila tuseme ni ipi au tendo lenyewe. Kisha tumuombe nguvu, ili tuanze njia mpya ya ushindi.

Tuelewe ni Mungu tu anayesamehe dhambi na si binadamu, hivyo tunapaswa kuungama dhambi zetu kwa Mungu. Na dhambi zingine huwezi kumwambia binadamu kabisa, ni Mungu tu. Ila unapomkosea mtu, nenda pia kwa mtu huyo ukamuombe msamaha.

Daudi alipofanya dhambi hizi alianza kuwa dhaifu. Alifanya watu wasimheshimu kama zamani. Hata mpwa wake Yoabu au watoto wake walipofanya uovu, aliogopa kuwaambia. Hivi ndiyo dhambi inavyoua furaha na uzuri wetu, inatufanya tuwe wanyonge, na inaharibu kila inachoshika. Na inafanya ushuhuda wetu kupungua

nguvu “Lakini, kwa kuwa kwa tendo hili umewapa adui za Bwana nafasi kubwa ya kukufuru, mtoto atakayezaliwa kwako hakika yake atakufa” 2 Samuel 12:14. Jambo la muhimu ni kwamba Mungu hutusamehe na kutusaidia tuanze ukurasa mpya usio na mawaa. ila tukirudia dhambi ile ile, inatufanya tukose nguvu ya kuishinda mara zingine. Mungu atusaidie na kutuokoa kutoka dhambini!

Tunapaswa kuja kwa Bwana kwa moyo mnyenyekevu, ulio tayari kufundishika. Sauti ya adui yetu ikisema, “umetenda dhambi, na huna haki ya kudai ahadi za Mungu”, tunapaswa kumwambia adui, “Imeandikwa, ‘Mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki’ (1 Yohana 2:1). Mwandishi wa Zaburi anasema, “Nalikujulisha dhambi yangu, wala sikuuficha uovu wangu. Nalisema, Nitayaungama makosa yangu kwa Bwana; Nawe ukanisamehe upotovu wa dhambi yangu.” Zaburi 32:5. Huu ndio aina ya uzoefu ambao tunapaswa kuwa nao.

Daudi alisamehewa kosa lake kwa sababu aliunyenyekeza moyo wake mbele za Mungu kwa toba na majuto ya nafsi yake, na kuamini kwamba ahadi ya Mungu ya kusamehe ingetimizwa. Aliungama dhambi yake, akatubu, na akaongoka tena. Katika kushangilia ule msamaha, alisema “Heri aliyesamehewa dhambi, ambaye dhambi yake imesitiriwa. Heri Bwana asiyemhesabia upotovu, Ambaye rohoni mwake hamna hila.” Zaburi 32:1, 2. Baraka huja kwa sababu ya msamaha; msamaha huja kwa njia ya imani, kwa kukiri na kuungama dhambi, na hiyo dhambi inawekwa kwa Yesu, Mbebaji dhambi mkuu. Baraka zetu zote hutoka Kristo. Kifo Chake ni dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. Yeye Ndiye Mpatanishi mkuu ambaye kupitia Kwake tunapokea rehema na upendeleo wa Mungu. Tusibebe hatia maisha yetu yote, tuungame na kujisamehe, Mungu anapotusamehe, na wale tuliowakosea kama kesi ya Daudi tulivyoona, tuwaombe msamaha pia.

Tunapofanya kazi kubwa ya kuendeleza kazi ya Mungu, kuna mambo mawili ya kuzingatia: Mungu atakuwa pamoja nasi na Shetani naye atakuwa pale ili kuipinga kazi ya toba ya kweli. Hata hivyo, hili halipaswi kuwa la kutuhangaisha sana kwa sababu Yeye aliye ndani ya mioyo yetu ni Mkuu zaidi ya Yeye aliye ulimwenguni.
*MUNGU WETU YUPO PAMOJA NASI, NA YUPO TAYARI KUTUSAMEHE NA KUTUSAIDIA KUISHI NDANI YAKE, HATA UKAMILIFU WA DAHARI, SWALI LANGU NI HILI: Je, mimi Nipo Pamoja NAYE? Ndiyo swali tunalopaswa kujiuliza kila siku!

*Pamoja na matibabu yetu yote tunayowapa wagonjwa, maombi rahisi na ya bidii yanapaswa kutolewa kwa ajili ya baraka za uponyaji. Tunapaswa kuwaelekeza wagonjwa kwa Mwokozi Mwenye huruma, na nguvu Yake ya kusamehe na kuponya.

---

Tungame dhambi zetu kwa nani? Tukimkosea mtu tufanyeje? Dhambi inaharibuje furaha yetu? Unafikiri Daudi aliwaomba watu gani msamaha? Masomo gani tunapata kutoka Zaburi 32 na 51? Taja sehemu 5 kwenye Biblia ambapo wameandika Mungu anasamehe dhambi?

**SIKU YA 94**
**(Aprili 3)**

# Uovu Nyumbani mwa Daudi

**- 2 Samweli 12-13**

Kisha Daudi alikwenda vitani. Yoabu alimwita aende kuutwaa Raba akisema "nisije mimi nikautwaa mji, ukaitwa jina langu." Aliendа akautwaa Raba na taji ya 11mfalme ya dhahabu ya kilo 34 yenye vito vya thamani ndani yake, akachukua na nyara nyingi, na watu akawaweka wawe watumishi kwenye kazi za misumeno, sululu, matofali na chuma.



Ikawa Absalomu mwana wa tatu wa kiume wa Daudi alikuwa na dada mzuri wa uso aitwaye Tamari. Naye Amnoni mwana wa kwanza wa Daudi akampenda dada yake wa baba mmoja na mama mbalimbali. Akaugua na kusononeka kwa mapenzi ya uovu. Tamari alikuwa hajaolewa, na Amnoni akaona ni vigumu kufanya lolote. Kwa desturi za siku zile, watu waliruhusiwa kuoa dada zao wa mama mwingine. Amnoni alikuwa na binamu na rafiki yake aliyeitwa Yonadabu, aliyempa wazo ovu. Alimwambia, "Kwa nini, Ee mwana wa mfalme, unakonda hivi siku kwa siku? Hutaki kuniambia?" Yonadabu aliyejulikana kwa ujanja, aliambiwa na Amnoni kwamba anampenda Tamari. Yonadabu akatoa njama ovu kabisa, akamwambia rafiki yake alale kitandani na kujifanya mgonjwa, na baba yake Daudi akija kumtazama, amwambie kwamba amlete Tamari, dada yake, apike mkate ili apate kula, ila apike machoni pake, akasema "nikakione, nikakile mkononi mwake." Basi akafanya hayo, na Daudi akamtuma Tamari binti yake kwa kaka yake Amnoni, naye akakanda unga na kupika na kumpa kaka yake mkate. Amnoni akawaambia watu wote watoke, na walipotoka alimshika dada yake kwa nguvu na kumwambia aje alale naye. Dada yake akamwambia, "La, sivyo, ndugu yangu, usinitenze nguvu, haifai kutendeka hivi katika Israeli; usitende upumbavu huu. Nami nichukue wapi aibu yangu? Basi, sasa, nakusihi, useme na mfalme; kwa maana yeye hatakukataza kunioa." Amnoni hakusikiliza shauri bali akawa na nguvu kuliko dada yake na akamtenda uovu. Ajabu, baada ya kumpata akamchukia machukio makuu. Na ile chuki yake ikashinda mapenzi yale aliyosema anampenda kwanza. Akamwambia "ondoka nenda zako." Tamari akasema sivyo, unavyonifukuza ni vibaya kuliko ulivyonifanyia. Akakataa kumsikiliza, na kumwita mtumishi akisema, "mtoe sasa mwanamke huyu kwangu,

ukafunge mlango nyuma yake." Hata leo watu wanadai kumpenda msichana na kusema, "sili, silali, nakuota wewe" na tunashangaa wanaotaje ndoto bila usingizi basi, na kisha  wakimpata au akiwa mke, wanamtendea uovu, na hawamjali na humwacha aende kwa aibu. Huu ni uovu.

Tamari akalia kwa sauti, na kujitia majivu kichwani, akararua mavazi yake marefu ya uanawali, na kuweka mikono kichwani. Kaka yake wa tumbo moja, Absalomu alimkuta na kumwuliza, naye alimweleza yaliyotokea naye akamtuliza, "tulia dada ni nduguyo usilitie moyoni." Jambo hili ni uovu mkubwa. Tamari alikaa hali ya ukiwa kwa kaka yake, Absalomu, kutokana na yale maovu aliyofanyiwa. Daudi alikasirika sana, ila kwa vile hata yeye alikuwa amefanya dhambi ya kumchukua mke wa watu kwa nguvu, alikosa nguvu kumwambia mtoto lolote. Basi Absalomu alikuwa na hasira, na alijua atalipiza kisasi kwa ajili dada yake, akamchukia Amnoni mno, na hakusema naye kwa shari wala kwa heri. Ni muhimu sana kufanya suluhu na dada au kaka zetu bila ya kuacha mambo yaende mbali kiasi hiki.

Baada ya miaka miwili, Absalomu alifanya karamu na kualika wana wa mfalme, na akamwomba baba yake aje na ndugu zake. Daudi alitoa udhuru kwa Absalomu akisema "tusiende sote tusije tukakulemea." Basi Absalomu akaomba ndugu yake Amnoni aende, naye mfalme akashangaa, "kwa nini aende nawe?" Akamsihi sana mfalme, mpaka akamwacha Amnoni aende naye. Absalomu akawaambia watumishi wake, Amnoni akilewa wampige na kumwua, na ndivyo walivyofanya. Wana wote wa mfalme walipoona hivyo wakakimbia. Mfalme akapata habari, kwamba Absalomu ameua wana wote wa mfalme na akararua nguo zake, na kulala chini. Yonadabu, mshauri aliyeanzisha uovu, akasema si wote wameuawa ila Amnoni, na sababu ni kutenzwa nguvu kwa umbu lake Tamari. Basi mfalme akapaza sauti akalia na wana wake. Absalomu akakimbia kwenda nchi ya Geshuri, kwa babu yake mzaa mama. Naye Daudi akawa amepotelewa na wana wawili sasa. Alikaa kule miaka mitatu, na mfalme akatamani amwone, kwa maana sasa alijua Amnoni ameshakufa. Alikuwa kama wazazi wengi, kiongozi mzuri kwa watu wengine ila nyumbani anashindwa kuongoza.

Ukosefu wa uadilifu, kulipiza visasi, na ufisadi katika visa hivi ni kama yale tunayaona kwenye runinga na majumbani mwa watu leo. Mvutano kati ya Abneri na Ishboshethi, Daudi na Abneri, Yoabu na Abneri, halafu kuna Daudi na wake zake wengi - ambao ni pamoja na Mikali, ambaye Sauli alimpa mtu mwingine, ingawa alipaswa kuwa mke wa Daudi kisheria. Msururu kama huo wa kasoro za tabia na malumbano ni moto wa kuotea mbali au jambo la kuepukwa kabisa! Tunapaswa kutambua kwamba Mungu hatukuzwi katika mambo haya ila neema Yake ya ajabu iko tayari kutusamehe na kuturudisha kwenye mstari tunapomruhusu kufanya hivyo. Visa hivi  siyo mfano wa ndoa ambazo Mungu anataka tuwe nazo. Lazima tukumbuke hata hivyo kwamba, hakuna mtu ambaye amewahi kuja kwa Kristo na ujuzi kamili wa kutekeleza maagizo Yake, na ndiyo sababu tunahimizwa kukua katika neema na katika maarifa ya Bwana na Mwokozi wetu. Cha muhimu ni kukumbuka kuwa Mungu hatuhukumu kwa nia zetu zisizofaa bali kwa subira hufanya kazi nasi ili kutufikisha kwenye ukamilifu.

Upendo wa Mungu ni wa ajabu kama nini! Baba tafadhali jaza moyo wangu na upendo huu, kwa kuwa Wewe pekee Ndiye uliye nao, na ninaweza kuwa nao tu ukinipa. Mwokozi wetu Mwenye upendo alikuwa tayari kufa kwa ajili ya wenye dhambi waasi, ili tupate fursa ya kuishi milele pamoja Naye. Daudi alimpenda sana mwanawe Absalomu lakini yeye alilichukulia kuwa jambo la kawaida, kama tunavyofanya katika uhusiano wetu na Mungu leo. Mpwa Yoabu kwa upande wake alikuwa mwanamkakati mahiri lakini mwenye ukatili. Alifanya kazi kulingana na viwango vyake na inaonekana kwamba hakumjali Mungu. Baba, tafadhali tusaidie kujifunza somo kutoka kwa maisha ya Daudi na Yoabu kwa sababu walikuwa wanadamu dhaifu kama sisi.

*Wale ambao hufanya kazi ya nyumba kwa nyumba watapata fursa za huduma katika namna nyingi (anuwai). Wanapaswa kuwaombea wagonjwa na wanapaswa kufanya yote katika uwezo wao kuwaondoa katika mateso.

---

Kwa nini Absalomu alienda Geshuri? Kwa nini Absalomu alimchukia Amnoni? Kwanini ni vyema kuepuka marafiki kama Yonadabu? Kwa nini Daudi alikosa nguvu ya kukanya wengine? Kwanini pombe ni kitu kibaya?

**SIKU YA 95**
**(Aprili 4)**

# Absalomu na Yoabu

**- 2 Samweli 14**

Basi Yoabu akajua kwamba mfalme amemkumbuka Absalomu kijana wake, na moyo wake ulitamani amwone. Yoabu alikuwa na mawazo ya busara pale alipopenda bali aliponuia uovu alibadilika. Safari hii Yoabu alijitahidi kuwa mpatanishi kwa kutenda lile lililo jema. Heri wapatanishi, kwani hii ni tabia ya Mungu, ambayo tunapaswa kuitenda, kwa kuupatanisha ulimwengu Naye. Basi Yoabu akatuma mwanamke wa Tekoa mwenye hekima aletwe kwake na kumwambia aende kwa mfalme na kuvaa nguo za matanga na kufiwa. "Nakusihi wala usijitie mafuta, ila ukafanane na mwanamke aliyeomboleza siku nyingi kwa ajili ya yeye aliyefariki. Akamwambia aende kwa mfalme na kumwambia hadithi. Basi yule mwanamke wa Tekoa aliendа kwa Daudi na kuanguka kifudifudi chini na kusujudia, akasema "Nisaidie Ee mfalme." Daudi akamwuliza una nini, maana kama mfalme enzi zile, alikuwa mwamuzi pia. Basi mwanamke yule akasema kuwa yeye ni mjane, alifiwa na mume, na alikuwa na wana wawili, nao walipigana na hapakuwa na wa kuwaamua, na mmoja akampiga mwenzake na kumwua. Jamaa wote wakainuka na kuja kwake wakisema amtoe yule aliyemwua mwenzake ili wamwue maana ndiyo adhabu ya mwuaji. Mwanamke wa Tekoa akasema kwa masikitiko kwamba wakimwua huyu ambaye ndiye mrithi aliyebaki, ndiyo "watakavyolizima kaa langu lililobaki" wasimwachie mume wangu jina wala masalio, usoni pa nchi. Mfalme akamwambia yule mwanamke aende nyumbani kwake, naye atamsaidia kesi yake, naye akasema, uovu huu uwe juu yake na si kwa mfalme wala kwa kiti chake cha enzi. Mfalme akasema wale wanaotaka kuja kumchukua kijana mrithi aliyebaki waende kwake, nao hawatamgusa mama huyu tena. Mama huyu kwa hekima akasihi tena kwamba aangalie "mlipiza kisasi asizidi kuharibu, wasije kumharibu mwanangu." Mfalme Daudi akamwakikishia "hautaanguka chini, hata unywele mmoja wa mwanao".

Ndipo mama huyu wa Tekoa akamsihi tena mfalme aseme neno moja tu, naye akasema "Kwa nini basi wewe umewafikiria mambo kama hayo watu wa Mungu". Kwa sababu mfalme hamleti Absalomu aliyemwua Amnoni. Akamsifia Daudi "Neno la bwana wangu mfalme na liwe la kustarehesha; kwa kuwa kama Malaika wa Mungu ndiyo alivyo bwana wangu mfalme, kuyapambanua yaliyo mema na yaliyo mabaya." Basi mfalme aligundua ni nani ametuma ujumbe kwake, na akamwambia mama wa Tekoa amwambie kama Yoabu ndiye yu pamoja naye katika hadithi ile yote. Yule mama akasema hawezi kugeuka kushoto au kulia maana Yoabu ndiye aliyemtuma, na kuweka maneno haya kinywani mwake. Akamwambia mfalme, "bwana wangu anayo akili, kama akili ya malaika wa Mungu, hata ajue mambo yote ya duniani." Basi mfalme akamwambia amrudishe Absalomu, na Yoabu akaanguka kifudifudi hata nchi akasujudu na kumbariki mfalme, akisema "mimi mtumwa wako najua ya kwamba nimepata neema machoni pako." Akaenda Geshuri na kumleta



Absalomu Yerusalemu ila akasema "ageukie nyumbani kwake, asinione uso wangu."

Daudi na mpwa wake Yoabu walikuwa na mahusiano ya kuogopana, kwani alimsaidia mfalme kufanya kazi zake mbovu. Daudi alijua pia kuwa Yoabu ni hodari wa vita, na msaada kwake kama Jemedari, ila alikuwa mtu wa Mungu hivyo falsafa yake haikuendana na ya mpwa wake Yoabu.

Tunaambiwa hakuna aliyekuwa na uzuri wa sura kuanzia utosi mpaka unyayo kama Absalomu. Nywele zake zilipendeza, na hata binti yake alikuwa mrembo, naye aliitwa Tamari. Absalomu alikaa miaka miwili, jumla mitano bila kumwona mfalme toka amwue kaka yake, Amnoni. Naye akatuma watu kumwita Yoabu binamu yake ili ampeleke kwa mfalme, lakini Yoabu alikataa kwenda. Kisha akawaambia watumishi wake wachome moto shamba la Yoabu. Ndipo akaenda nyumbani kwa Absalomu na kumuuliza kwa nini watumishi wamechoma shamba lake, naye akamwambia kuwa amemletea toka Geshuri, lakini hampeleki kwa mfalme, afadhali angemwacha kulekule. Akasema ni bora aone uso wa mfalme au mfalme amwue. Yoabu akazungumza na mfalme, naye Absalomu akaja kwa mfalme na kuanguka kifulifuli mpaka chini, naye mfalme akambusu.

Baada ya upatanisho na mfalme, Absalomu akaweka gari na farasi na watu 50 wakipiga mbio mbele yake. Akaondoka asubuhi na mapema na kusimama kando ya lango la mfalme. Akazungumza na wale waliokuwa na neno ambalo lilikuwa limfikie mfalme kwa kuamua mashauri au kupata hukumu.
Ombi la kila mzazi:

**OMBI LA MZAZI na AHADI (PLEDGE)**
Mtakatifu Mwenyezi Mungu nimezidiwa na majukumu ya uzazi wewe usipokuwa karibu nami juhudi zangu zitakuwa bure. Nakusifu kwa vile Wewe Ndiye chemchemi ya furaha, ushindi, shukurani, na yote mema katika maisha yangu. Asante kunipa watoto, ni mbaraka mkubwa. Nisaidie Baba kulea watoto wangu katika mpango wako japo sifai na ni mwenye madhaifu mengi. Nisaidie nisiwatukane na kuwakatisha tamaa kwa kuwaita majina ya ovyo na kuwaaibisha. Nisaidie niwatie moyo kwa yale mazuri wanayofanya na kuwakumbatia nikiwazingira kwa maneno ya kuhuisha nafsi. Ninaelewa kabisa kwamba kutokana na tabia yangu haya si rahisi! Nisaidie nishike hatamu ya ulimi wangu wakati ambapo napaswa kusikiliza badala ya kubwatika. Naomba niweze kuwasikiliza pale wanaponihitaji. Unisaidie nisiwasakame sakame. Nirekebishie sauti yangu wakati ambapo nawaadabisha. Niweze kuwa mvumilivu, kuwasaidia wawe na tabia njema na kuweza kuwa watu

wa kukabiliana na majukumu yao. Naomba hekima ili nisidai wafanye vile ambavyo haviwezekani au ambavyo mimi mwenyewe sivifanyi. Naomba pia nisiwadekeshe, kwa vile nasikia hatia ya kutokuwa nao muda mrefu, na kisha nawaachilia wafanye wapendavyo, ili wanipe nafasi nijifanyie mambo yangu, na kuwa mtandaoni masaa mengi.

Naomba niwe na tabasamu kwenye uso wangu. Hebu nyumba yetu ijae furaha na vicheko. Nisaidie nijue wakati wa kuacha kazi kando na kufurahia maisha na watoto. Naamini utanisaidia kujenga nyumba ya furaha na kumbukukumbu njema kwa watoto wangu ambayo itaendelea hata kwa wajukuu wangu.

Nisamehe kwa mapungufu na dhambi ambazo nimezifanya siku za nyuma kuhusu malezi yao. Nisaidie niwasamehe watoto pia. Nisaidie niachane na hasira, manunguniko, wivu, dhamira ya kunishitaki, na chuki ambayo itafanya nisiwasaidie watoto. Naomba unisaidie niwaonyeshe upendo toka udogo mpaka utu uzima. Hebu wajue upendo kwa sababu wameupata hapa nyumbani. Naomba nisiwalinganishe na watoto wa jirani zangu, bali nipokee ahadi Zako, na kuzitumia kwa watoto wangu. Watoto wangu ni watoto Wako baba. Nawakabidhi kwa mkono hodari. Hebu mfano wangu wa kukupenda na kukutumikia ukawe wao, ili wapende kukutumikia Wewe milele na watu ambao wana mahitaji. Nisaidie kujenga tabia Yako ndani yao, ambayo ndiyo pekee watayokwenda nayo mbinguni na wala si magari, nguo au mashamba. Tujaze Roho Wako Mtakatifu ili tusiwe na tamaa mbaya za vitu au uovu. Tusaidie nyumbani kwetu, tuyasalimishe mapenzi yetu Kwako.

Naomba kuliko yote unisaidie uvumilivu wa kujitawala nafsi. Baba sikufundishi kuomba, bali wewe wajua mimi na watoto tunachohitaji kuliko yote kwa malezi bora. Asante kwa vile unaenda kutenda zaidi ya yale niliyokuomba au kufikiri. Nakupenda Mungu wangu, na asante kwa kuwa unajibu maombi kwa maisha ya mbeleni ya hawa watoto. Naamini utatusaidia mahitaji yetu yote katika wakati uliopanga.
Amina

Tarehe------------------------

Jina----------------------------

*Mwokozi angetutaka tuwatie matumaini wagonjwa wasio na tumaini, walio na shida ya maumivu au mateso, kushikilia nguvu Zake. Kupitia imani na maombi chumba cha wagonjwa kinaweza kubadilishwa kuwa Betheli (nyumba ya Mungu kama pale Yakobo alipita).

---

Mwanamke wa Tekoa alitoa kisa gani? Ni nani alimtuma mwanamke huyu aende kwa mfalme? Kwa nini Daudi hakuwa na muda wa kulea watoto wake vyema? Kwa nini Absalomu alichoma shamba la Yoabu? Je, uzuri wa uso au mwili unawezaje kuwa kikwazo kwa maisha yetu? Kwanini wazazi hupenda watoto wao hata wanapokosea?

**SIKU YA 96**
**(Aprili 5)**

# Matamanio Yasiyo Matakatifu na Yenye Ubinafsi

**- 2 Samweli 15**

Daudi alihusika na shughuli za uongozi za kifalme kama kuwa hakimu, kwenda vitani na hata kutunga nyimbo. Kwa namna fulani, aliacha mwanya ambao Absalomu aliutumia kwa manufaa yake.

Absalomu aliita watu waliokuwa wanaenda kwa mashauri kwa baba yake na akawauliza wanatoka mji na kabila lipi. Naye akasikiliza shida zao langoni na kuwaambia, “maneno yako ni mema yenye haki, lakini hapana mtu aliyeagizwa na mfalme kukusikiliza.” Akawaambia ingekuwa yeye ndiye mwamuzi katika nchi na kila mtu mwenye kesi aje kwake, basi angempa haki kila mtu na wangefurahia uamuzi wake. Na watu walipomkaribia na kumsujudia, alinyosha mkono wake, na kumshika mtu huyo na hata kumbusu. Aliwatendea hivyo wale waliomwendea mfalme kupata hukumu, na hivyo akawadanganya watu wa Israeli, na kugeuza mioyo yao kwake kutoka kwa baba yake. Baada ya miaka minne, alimwambia mfalme amwache aende kuondoa nadhiri yake aliyomwekea Bwana akiwa Geshuri kwamba akirudi ndipo, “atamtumikia BWANA.” Mfalme akamwambia aende kwa amani naye akaondoka kwenda Hebroni.

Alipofika kule alifanya kwa hila kupeleka wapelelezi katika Israeli kwa kabila zote  na kuwaambia watakaposikia tarumbeta, waseme, “Absalomu anamiliki huko Hebroni.” Watu 200 walioalikwa wakatoka kule pamoja na Absalomu, wakaenda katika ujinga huo wa Absalomu, wasijue neno lolote. Absalomu akamwita Ahithofeli, mshauri wa Daudi na babu wa Bath-sheba alipokuwa akitoa dhabihu. Yeye na Absalomu wakaendelea na fitina ya kutaka kumpindua Daudi. Pengine Ahithofeli, hakupenda jinsi Uria alivyofanyiwa, alimradi wakaungana na Absalomu, japo yeye alikuwa mwenye hekima na mzee zaidi.

Mtu mmoja alikwenda na kumwambia Daudi, “mioyo ya watu wa Israeli inashikamana na Absalomu”, basi akajua Absalomu anakuja kuwadhuru ili achukue ufalme. Naye akawaambia watumishi wake wote wakimbie na kuondoka mjini, kwani wasipokimbia, hakuna atakayeokoka mikononi mwa Absalomu. Wakakimbia upesi, kabla Absalomu hajaleta uovu wake, na kuwapiga kwa makali ya upanga. Watumishi wake wakawa tayari kufanya lile Daudi alilowaambia; basi akatoka na watu wa nyumbani kwake wote isipokuwa masuria kumi wakaachwa ili kutunza nyumba. Walipotoka walikaa kidogo Beth-merhaki, kisha wakapita karibu naye watu 600 walioandamana naye kutoka Gathi. Mfalme akamwambia Itai Mgiti kwa nini aende pamoja nao; akamsihi arudi aende pamoja na Absalomu mfalme mpya. “Kwa kuwa umekuja jana tu kwa nini nikusumbue leo, na kukuzungusha

huko na huko pamoja nasi nami naenda niwezapo kwenda." Akamwambia arudi na kurudisha nguvu zake, akamtakaia rehema na kweli ziwe pamoja naye. Naye Itai akamjibu mfalme akasema, Kama aishivyo BWANA na bwana wangu mfalme aishivyo, hakika yake kila mahali atakapokuwapo mfalme, nami nitakuwapo, ikiwa ni kwa kufa au ikiwa ni kwa kuishi, ndipo atakapokuwapo na mtumwa wako. Basi mfalme akamwambia wavuke pamoja, na watoto pia wakavuka. Nchi ikalia kwa sauti kuu, na watu wakavuka, na mfalme kijito cha Kidroni wakielekea njia ya nyika. Sadoki kuhani akaja na Walawi na sanduku la agano, kuonyesha uaminifu wake kwa mfalme, Abiathari kuhani naye akapanda juu mpaka watu wote walipomaliza kutoka mjini. Ndipo mfalme alipomwambia Sadoki arudi na sanduku la Mungu na akasema, "nikipata kibali machoni pa Bwana atanirudishia na kunionyesha tena sanduku hili na masikani yake; lakini akisema si radhi nawe kabisa basi mimi hapa, na anitendee kama aonavyo kuwa vyema." Akamwambia arudi na wana wake wawili wa makuhani, yaani, Ahimaasi mwana wa Sadoki na Yonathani mwana wa Abiathari.

Daudi akasema ataondoka kwenye vivuko vya jangwani na atasikia toka kwao kuhusu habari ya mambo ya mapinduzi ya Absalomu yanavyoendelea. Sadoki na Abiathari walichukua sanduku la BWANA wakarudi Yerusalemu. Daudi akapanda njia ya mlima wa Mizeituni akilia alipokuwa akipanda na akiwa amejifunika kichwa chake na bila kuvaa viatu. Watu waliomfuata walijifunika vichwa pia na wakapanda juu wakilia. Mtu mmoja akamwambia Daudi kwamba Ahithofeli ndiye mpendwa na mshauri wa Absalomu, naye akaomba akisema, "Ee Bwana nakusihi uligeuze shauri la Ahithofeli liwe ubatili." Ikawa alipofika juu, mahali pa ibada, alimwona Hushai akija kumlaki, na joho lake limeraruliwa tena ana udongo kichwani mwake. Daudi akamwambia Hushai, akija pamoja naye atakuwa mzigo kwake, ila akirudi mjini na kumwambia Absalomu "nitakuwa mtumishi wako, kama nilivyokuwa mtumishi wa baba yako, ndipo utakapovunja mashauri ya Ahithofeli kwa ajili yangu." Akamwambia makuhani wote wawili, Sadoki na Abiathari wako huko na wana wao, na kwa kupitia wana wao Ahimaasi na Yonathani mtanipelekea habari ya kila neno mtakalolisikia. Basi Hushai rafiki wa Daudi akaingia katika mji naye Absalomu akaingia Yerusalemu.

Absalomu aliiba mioyo ya watu kwa udanganyifu sawa na vile Shetani alivyofanya mbinguni, na kwa sababu ya upendo Wake kwa mwanawe, Daudi alikimbia ili kuepuka kumwaga damu. Tamaa na kiburi vilimsukuma Absalomu kutojali maisha ya wengine. Masomo haya yasikike mioyoni mwetu tunapopitia njia hii. Daudi alikuwa jasiri katika saa yake ya dhiki, na mkarimu kwa maneno yake. Hili ni jambo jema kwetu kujifunza.

*Ikiwa tuna udhaifu wa mwili, kwa kweli ni sawa kumtumainia Bwana, tukiomba dua kwa MUNGU wetu katika kesi yetu, na ikiwa tunajisikia kuwaomba wengine ambao kupitia wao tunao ujasiri wa kuungana nao kwa ajili ya maombi kwa Yesu ambaye ni Tabibu hodari, hakika msaada utakuja ikiwa tutaomba kwa imani.

---

Absalomu alibadilishaje mioyo ya watu toka kwa babaye? Kwa nini Daudi alikimbia

toka Yerusalemu? Kwa nini Daudi hakutaka kuchukua marafiki zake kama Hushai? Kwa nini Daudi hakutaka kulichukua sanduku la Agano? Ahithofeli alikuwa ni nani? Kwanini watu huwa na washauri? Unachaguaje washauri wako?

**SIKU YA 97**
**(Aprili 6)**

# Absalomu Afanya Vita na Babaye

**- 2 Samweli 15-18**

Daudi alipopita kilele cha mlima, akamwona Siba mtumwa wa Mefiboshethi anamfuata na punda wawili waliotandikwa na mikate 200, vishada vya zabibu, matunda, na viriba vya divai. Daudi akamwuliza, vitu hivi ni vya nini? Naye akajibu punda, na chakula hiki ni kwa mfalme na vijana, wale wazimiao nyikani. Akamwuliza bwana wake Mefiboshethi yupo wapi? Naye akajibu, amemwacha Yerusalemu, maana alisema pengine leo Israeli watamrudishia ufalme wa baba yake Yonathani. Mfalme akaona Mefiboshethi hana uaminifu, ila Siba, na akamwambia yale yote aliyomwahidi Mefiboshethi yawe ya Siba, na Siba akasujudu na kusema, "Nione kibali machoni, pako Ee bwana wangu mfalme. Mfalme alipofika Bahurimu, akamwona Shimei, jamaa ya Sauli akilaani alipokuwa akienda, na kumtupia Daudi mawe na watumishi, na mashujaa wa Mfalme Daudi waliomzunguka kushoto na kulia. Shimei akamlaani akisema, "Nenda zako! Nenda zako Ewe mtu wa damu! Ewe mtu usiyefaa. Bwana amerudisha juu yako damu yote ya nyumba ya Sauli ambaye umetawala badala yake Naye BWANA ametia ufalme katika mkono wa Absalomu mwanao kwa ajili ya uovu wako mwenyewe kwa sababu umekuwa mtu wa kumwaga damu za watu. Abishai akamwambia mfalme, Mbona mbwa mfu huyu amlaani mfalme na bwana wangu, nivuke, nakusihi, nikaondoe kichwa chake." Ila mfalme akamwambia amwache tu kwa sababu yeye analaani, na kwa sababu BWANA amemwambia mlaani Daudi, basi ni nani atakayesema mbona umetenda haya?" Daudi akawaambia watumishi wake, mtoto wake aliyemzaa mwenyewe Absalomu anatafuta uhai wake "si zaidi Mbenyamini huyu sasa, mwacheni alaani, kwa sababu BWANA Ndiye aliyemwagiza; pengine BWANA ataangalia mabaya yaliyonipata, Naye atanilipa mema kwa sababu ya kulaani Kwake leo. Waliendelea kupanda ubavu wa kile kilima, naye Shimei aliendelea kulaani, akitupa mawe na mavumbi, naye mfalme na watu aliofuatana nao wakafika wamechoka, wakapumzika huko.



Absalomu na watu wote waliokuwa pamoja naye wakafika Yerusalemu na Ahithofeli

mshauri. Hushai rafiki wa Daudi alipomjia Absalomu na kumwambia "aishi mfalme". Absalomu akaona kama amemsaliti Daudi babaye na akamwambia Hushai, "Je! Huu ndio wema wako kwa rafiki yako?" mbona hukwenda pamoja na rafiki yako. Naye Hushai akamwambia, atamtumikia yeyote yule ambaye BWANA amemchagua, na kukaa Naye au kumsaidia. Akasema Daudi ni rafiki yake, na ndiyo maana "hainipasi kutumika mbele ya mwanawe, kama nilivyotumika mbele ya baba yako, ndivyo nitakavyokuwa mbele yako." Absalomu akaomba mashauri kwa Ahithofeli, wafanye nini. Naye Ahithofeli akatoa ushauri wa uovu, kwamba awachukue wale masuria wa baba yake, na hilo litaonesha watu kwamba amechukizwa kabisa na baba yake, ili wale wanaofuatana naye wajue wazi, na hii pia itaonesha kuwa yeye ndiye mtawala.

Basi Absalomu akafuata ushauri huu wa kipumbavu, huku watu wa Israeli wakishuhudia. Watu wengi walichukulia ushauri wa Ahithofeli kama ushauri wa Mungu siku zile, hata alipomshauri Daudi, alionekana ana hekima. Naye Ahithofeli akasema achague watu 12,000 na kumfuatia Daudi usiku ule ule, kwa vile amechoka na ni dhaifu, naye atawatia hofu watu wote walio pamoja naye wakimbie, ili ampige mfalme Daudi peke yake. Kisha awarejeze watu wote wawe upande wake. Shauri hili likawa jema machoni pa Absalomu na wazee wa Israeli, ila Absalomu akasema Hushai ni mshauri pia hivyo naye aitwe wasikie anayotaka kusema. Hushai akaona hili litamwangamiza mfalme Daudi, naye akasema la! "wamjua baba yako na watu wake, ya kuwa ni watu mashujaa hawa nao wana uchungu katika mioyo yao, kama dubu aliyenyanganywa watoto wake nyikani. Tena baba yako ni mtu wa vita, hatalala pamoja na watu wake. Angalia amefichwa sasa katika shimo… hata yeye aliye shujaa mwenye moyo kama wa simba atayeyuka kabisa. Hushai akashauri Waisraeli watoke wakusanyike kwake Absalomu kisha, aende vitani mwenyewe, na wamfikie na kumwangukia kama vile umande uangukavyo, wasiache mtu yeyote aliye pamoja naye. Basi watu wakasema ushauri wa Hushai ndiyo mzuri kuliko wa Ahithofeli. Hawakujua kuwa BWANA amekusudia kulivunja shauri jema la Ahithofeli, ili kumwokoa Daudi mtumishi wake na kuleta mabaya kwa mwovu Absalomu. Hushai akawapa ujumbe Abiathari na Sadoki makuhani, ujumbe wa mashauri aliyotoa na pia yale Ahithofeli aliyotoa. Akawaambia wampelekee Daudi ujumbe, kwamba asilale usiku ule karibu na vivuko vya jangwani, bali avuke, asije akamtweza na watu wote walio pamoja naye.

Yonathani na Ahimaasi walipata ujumbe na kwenda kumwambia mfalme Daudi, bila kuonekana wakiingia mjini. Ila kuna kijana mmoja aliwaona vijana hawa wawili, bahati nzuri waliingia katika nyumba ya mwanamke aliyekuwa na kisima na akawafunika ndani ya kisima, na Absalomu alipotuma watu kumwendea yule mwanamke na kuuliza Ahimaasi na Yonathani wako wapi, yule mwanamke akasema "wamevuka kijito cha maji." Walipowatafuta wasiwaone walirudi Yerusalemu. Nao wakatoka kisimani na kumwarifu mfame Daudi. Naye akawaambia waondoke upesi kuvuka maji. Basi walivuka Yordani wote waliokuwa na Daudi. Naye Ahithofeli alipoona ushauri wake haukufuatwa alijua kuwa Daudi atarudia ufalme, naye kwa vile ni msaliti atapata adhabu, basi alipanda punda wake, akaenda nyumbani kwake, akaweka mambo yake sawa, kisha akajinyonga na kufa. Absalomu naye akavuka Yordani na Israeli, na akamweka Amasa Mwishmaeli kuwa amiri jeshi

wake. Daudi akaenda Mahanaimu na watu wakaleta magodoro, vyungu, shayiri, mabakuli, ngano, kunde, dengu, asali, siagi, kondoo, samli, na ng'ombe ili wapate kula maana walikuwa na njaa, kiu na kuchoka. Daudi akaweka viongozi wa elfu elfu na mia mia. Na akawapeleka watu vitani, chini ya mkono wa Yoabu, Abishai na Itai. Kila mahali tunaona familia zilizovunjika, kama familia ya Daudi. Watu wanahitaji uponyaji. Watu wanahitaji matumaini. Absalomu alikuwa kijana muasi asiye na udhibiti ambaye alikuzwa bila kuadabishwa vyema, pengine kwa vile watoto walikuwa wengi na baba alikuwa na shuguli nyingi. Hili ni onyo kwa wazazi na mabibi na mababu wanaowapenda watoto kwa kupitiliza, hata wanakuwa wapofu pale wanapokosea. Kupuuza tabia za watoto ziliishia kumsababishia maumivu makali. Katika kisa cha Absalomu malalamiko tunaona yasiposhughulikiwa, husababisha uchungu, chuki na hasira ambayo mwishowe inaleta uharibifu. Tafadhali utusaidie Bwana kukabiliana na dhambi mara moja kabla haijaota mizizi na kutuangamiza. Upendo wa mzazi unaweza kufananishwa na upendo alio nao Mungu kwa kila mmoja wetu. "Mungu amenyesha pendo Lake Yeye Mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi." Warumi 5:8. Baada ya kulipia gharama ya dhambi zetu, anatuuliza: "Njoni sasa, tusemezane," asema Bwana, "zijapokuwa dhambi zenu ni nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama nyekundu, zitakuwa kama sufu." Isaya 1:18 NKJV. Kwa hiyo, haijalishi dhambi zetu ni kubwa kiasi gani, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yohana 1:9.

*Tulituma maombi yetu ya unyenyekevu kwa ajili ya yule aliye mgonjwa na aliyesumbuliwa, ambaye alikuwa njiani kupoteza maisha haya. Tulipowasilisha jambo hii mbele ya Bwana, tulihisi uhakikisho wa upendo wa MUNGU hata katika shida hii.

---


Ahithofeli alitoa ushauri gani? Maamiri jeshi watatu wa Daudi walikuwa nani? Kazi ya Ahimaasi na Yonathani ilikuwa ipi? Nani alifichwa kwenye kisima cha maji na mwanamke? Makuhani wawili walikuwa nani? Shimei alisema maneno gani? Absalomu alitaka nini toka kwa babaye? Mtu akiwa na shida kubwa kwanini kujinyonga siyo kabisa ufumbuzi wa suala hata ukichukuliwa kwamba sisi si mali yetu wenyewe?

**SIKU YA 98**
**(Aprili 7)**

# Absalomu Auawa

**- 2 Samweli 18-19**

Daudi akawa tayari kwenda kupigana na watu wake, ila watu wakamwambia asitoke, maana wao wakikimbia, watu hawatajali sana ila yeye akikimbia watamfuata. "Wewe u wa thamani kuliko watu elfu kumi katika sisi." Wakasema asikie na kukaa mjini na kushughulikia mambo pale. Mfalme akakubali na kuona yaliyo mema machoni kwao ndiyo atafanya. Jambo zuri, ni kwamba mfalme mcha Mungu, na nabii alikuwa na thamani machoni pa raia wake pia. Mfalme akasimama mlangoni watu wakienda vitani na majemedari watatu walipokuwa kwenye gwaride, kama baba, akamkumbuka mwanawe japo yeye hakumjali na alikuwa tayari kumwangamiza. Akaagiza, "mtendeeni yule kijana Absalomu kwa upole kwa ajili yangu," kweli upendo wa baba ulikuwa ni mzito, je, Mungu si zaidi? Watu wakaenda kupigana, vita vikatokea kwenye msitu wa Efraimu, na Waisraeli wakapigwa na jeshi la Daudi kwa maangamizo makuu, siku hiyo watu 20,000 wakafa. Vita vikapamba moto usiku wote na wengi wakafia msituni. Kwa bahati Absalomu akakutana na mtumishi wa Daudi naye alikuwa amepanda nyumbu, naye akapita chini ya matawi manene ya mwaloni, hata kichwa chake kikakwama katika mwaloni huo, naye akanyakuliwa mwili wake wote na shingo yake ikagota kwenye mti.



Basi alikuwa katikati ya mbingu na nchi, na mtu mmoja aliyeona hilo alienda na kumwambia Yoabu, maana aliogopa kumtenda lolote, kutokana na agizo la mfalme. Bali Yoabu ambaye pia inaonekana kuwa alimchoka Absalomu na alikuwa ana kisasi naye, alimwambia yule mtu mbona "hukumpiga hata nchi papo hapo? Nami ningalikupa fedha kumi na mshipi." Yule mtu akamkumbusha Yoabu, amiri na mpwa wa mfalme maagizo ya mfalme, na kwamba hata angempa fedha elfu, asingenyosha mkono wake kwa kijana wa mfalme, maana walipata maagizo na wote wanajua. Yoabu akasema hawezi kungoja wazungumze hadithi nyingi, akachukua mikuki mitatu na kumchoma Absalomu binamu yake moyoni, akali hai na kichwa chake kikiwa kimekwama kwenye mti. Kisha Yoabu akapiga tarumbeta ya ushindi, na wakarudi watu toka kuwafuatia Waisraeli, kwa maagizo ya Yoabu. Wakamtupa Absalomu msituni, kwenye shimo kubwa. Basi Ahimaasi mwana wa Sadoki akataka apige mbio kumwambia mfalme habari jinsi "BWANA alivyomlipiza kisasi juu ya adui Zake." Yoabu akamwambia yeye hatakuwa mchukua habari siku

ile, ila siku nyingine…. maana mwana wa mfalme amekufa.

Kisha Yoabu akamtuma mkushi aende kumwambia mfalme yale aliyoyaona. Mkushi akainama mbele ya Yoabu kama ishara ya kuyatenda aliyoagizwa na inaonekana alikuwa mtu wa hekima anapozungumza, na asiye na wasiwasi au harara. Ahimaasi mwana wa Sadoki, akarudi kusihi naye aende, hata kama akiwa mjumbe wa pili nyuma ya mkushi. Yoabu akashangaa kwa nini anakazana, kwani atapata nini kwa habari anazopeleka? Ila Ahimaasi akasema, haidhuru atapiga mbio, basi Yoabu akamkubalia na akapiga mbio. Akishika njia ya uwandani, pengine ya mkato, au alikuwa na mbio zaidi, akampita yule mkushi. Daudi alikuwa ameketi karibu na lango kuu, na mlinzi aliye darini akaona mtu anakuja mbio peke yake na akamwambia mfalme. Mfalme akajua, kama yupo mwenyewe ana habari, kisha mlinzi akaona mtu wa pili, anakuja akikimbia, na mlinzi akasema yule wa kwanza ni kama Ahimaasi mwana wa Sadoki kuhani. Basi kwa vile mfalme alizoea Ahimaasi alikuwa mtu wa kuleta ripoti njema, alimwambia mlinzi "anakuja na habari njema." Ahimaasi akafika na kuinama kifudifudi, na kusema ahimidiwe BWANA Mungu wako, aliyewatoa watu hao walioiinua mikono yao juu ya bwana wangu mfalme. Mfalme kama baba aliyempenda mwanawe akauliza habari za Absalomu bila kuchelewa, "Yu salama?" Ahimaasi alishindwa kujibu akisema Yoabu alipomtuma aliona kishindo kikubwa ila hakujua sababu yake.

Basi mfalme akaona habari si kamili, naye akamwambia ageuke na kusimama akingoja mjumbe wa pili aje. Basi mkushi akaja na kusema, "Nina habari mfalme kwa maana BWANA amekulipizia kisasi leo juu ya hao wote walioinuka kupigana nawe." Mfalme akauliza usalama wa kijana wake. Ndipo mkushi akajibu kwa hekima kubwa, "adui za bwana wangu mfalme, na wote wainukao ili kukudhuru, na wawe kama alivyo yule kijana." Mfalme akasononeka kwa huzuni, akapanda juu na kuingia kwenye chumba chake akalia, akisema "mwanangu Absalomu! Ee! Mwanangu! mwanangu Absalomu! Laiti ningalikufa badala yako, Absalomu mwanangu, mwanangu." Kweli upendo wa baba ulikuwa ni mkubwa, na huu ni mfano wa Mungu atupendavyo japo tunamkosea mara kwa mara. Yoabu akamkanya mfalme anavyomlilia na kumwomboleza mwanae aliyemwasi, na kutaka kumwua. Maana kushinda vitani kwao kukawa maombolezo badala ya shangwe, walivyosikia mfalme akihuzunikia mwanawe. Watu wakajificha kama vile wanaona aibu au fedheha wakikimbia vita. Mfalme akajifunika usoni na kuendelea kulia, basi Yoabu akaenda kwake na kumwambia, "Wewe leo umefedhehesha nyuso za watumishi wako wote waliokuokoa leo roho yako, roho za wanao, wakezo, masuria na watu wote. Unawapenda wakuchukiao na kuwachukia wanaokupenda", akamwambia mfalme matendo yake yametangaza kwamba viongozi na watumishi aliowaweka si kitu, na kwamba wangekufa wote siku hiyo na Absalomu aishi ingekuwa furaha kwake. Akamwamrisha mfalme, "basi sasa, ondoka, utoke nje ukaseme na watumishi wako maneno ya kuwatuliza roho zao maana hatabaki hata mmoja upande wako usiku huu, na mambo yatakuwa mabaya kwako kuliko yote yaliyokupata toka ujana wako hata sasa."

Basi Mfalme akajikaza na kutoka langoni na watu wakaenda wamsikilize, baada ya kukimbia mahemani. Maana hata wale waliomfuata Absalomu walibaki kama

hawana uongozi mfalme akilia, wakajiwazia "mbona hamsemi neno lolote juu ya kumrudisha tena mfalme. Mfalme akatuma makuhani wawili na kusema na watu wa Yuda kwa nini wamechelewa kumwita mfalme arudi Yerusalemu. Basi hata Amasa Jemedari wa Absalomu akasema yuko pamoja naye, akawapatanisha watu wote wa Yuda hata wale waliomfuata Absalomu. Watu wa Yuda wakaja kumlaki mfalme na kumvusha Yordani. Shimei yule aliyemlaani Daudi, akaja amebadilika na kumlaki Daudi, na watu wa Benyamini kama Siba walikuwa naye, wakavuka Yordani. Shimei akamwangukia Daudi amsamehe, "usiyakumbuke yale niliyotenda mimi mtumwa wako kwa upotoe siku ile." Akamwambia mfalme asiyatie moyoni, kwani amekosa na sasa naja kumlaki bwana wangu. Abishai akasema auawe kwa kumlaani mfalme, ila Daudi akasema hakuna Israeli atayeuawa maana yeye ndiye mfalme na hiyo ni siku ya furaha, akamwapia Shimei kwamba hatakufa.
Daudi alitamani kufa badala ya Absalomu. Muumba wetu Yeye hakutaka tu kufa kwa ajili yetu, bali alikufa badala yetu. Je, alikufa lini kwa ajili yetu? Tulipokuwa bado tungali tunatenda dhambi dhidi Yake, Yeye alikufa kwa ajili yetu tukiwa bado maadui Zake kama vile Absalomu alivyokuwa adui wa baba yake. Ikiwa jitihada za Absalomu za kutaka kumuua hazingeweza kumzuia Daudi asimpende, ni nini kingeweza? Hakuna kitu! Vilevile, hakuna jambo tunaloweza kufanya ili kumfanya Mungu aache kutupenda. Hata tulipomsulubisha akiwa hai, bado alituombea akisema, "Baba uwasamehe kwa kuwa hawajui watendalo."Wenye dhambi wasiotubu watakapoishia katika moto wa jehanum baada ya hukumu ya upelelezi (kwa sababu Mungu ataheshimu maamuzi yao), Yeye atawalilia, kwa sababu hata katika wakati huo bado atakuwa anawapenda, kwa maana anasema, "Sifurahii kufa kwake mtu mwovu" (Ezekieli 33:11).

*Tulimuweka wakfu mtoto na kuomba juu yake, tukiamini kwamba Bwana atawapa mama na mtoto amani. Ikawa hivyo. Kilio cha mtoto kilikoma, na tukawaacha wakiendelea vizuri.

---

Kwa nini watu walikataa Daudi asiende vitani? Absalomu alifanya kosa gani? Je, baba yake alimpenda bado? Unajuaje kama alimpenda? Shimei alifanya kosa gani? Daima Mungu ana rehema na tumaini linalobubujika, je umeliona hili kwenye maisha yako?

**SIKU YA 99**
**(Aprili 8)**

# Daudi Arejea Katika Ufalme

**- 2 Samweli 19-21**

Mefiboshethi mwana wa Sauli akashuka amlaki Daudi, akiwa hakukata kucha na ndevu za miguu yake hazijakatwa. Wala hajafua nguo zake toka mfalme ameondoka mpaka aliporudi kwake kwa amani. Mfalme akamwuliza mbona hakuja pamoja naye, ndipo alisema yeye ni kiwete "lakini bwana wangu mfalme ni kama Malaika wa Mungu; utende basi yaliyo mema machoni pako." Kwa kuwa jamaa zake walikuwa watu wa kufa mbele ya mfalme, ila amewapenda na kuwaweka mezani pake, hivyo alisema hana haki ya kuuliza zaidi. Naye mfalme akasema wagawane na Siba ile ardhi, naye Mefiboshethi akasema, hata Siba akitwaa yote, yeye hatajali, jambo la muhimu ni kwamba, mfalme amerudi kwa amani nyumbani kwake. Barzilai mgileadi akaja na kuvuka Yordani, naye alikuwa mzee wa miaka 80, na alikuwa amefanya kazi ya kumlisha mfalme, na alikuwa mtu wa cheo kwenye himaya ya Daudi. Mfalme akamwambia Barzilai wavuke kwenda kuishi pamoja Yerusalemu, naye atamtunza huko. Lakini Barzilai alisema ana siku chache, kupanda na mfalme kwenye ikulu; "nimepata leo miaka 80, Je! naweza kupambanua mema na mabaya?" Akasema hata ulimi wake hauwezi kuonja chakula vizuri kwa uzee, na hata kusikia sauti za kwaya nzuri za mfalme tena. Akasema hataki kumpa shughuli nyingi mfalme, akashukuru kwa thawabu anayopewa na mfalme, ila amwache arudi kwenye mji wake, karibu na makaburi ya wazazi wake. Akaomba mtumwa wake Kimhamu aende badala yake "ukamtendee yeye yaliyo mema machoni pako." Basi mfalme akakubaliana na hilo, akamtwaa Kimhamu. Watu wote wakavuka Yordani na mfalme akambusu Barzilai na kumbariki, kisha akarejea kwake.

Watu wa Yuda wakaanza kugombana na Israeli na Sheba mtu asiyefaa kitu akapiga tarumbeta na kusema kwamba anatangaza ufalme wa kabila lake la Benyamini. Watu wa kabila lake wakamfuata, ila watu wa Yuda wakaambatana na mfalme. Walipofika Yerusalemu walikuta wale wanawake kumi masuria, nao walikuwa hai walipoachwa, ila toka siku ile hawakuwa masuria wa mfalme tena bali walitunzwa na mfalme.

Mfalme akamwambia Amasa, aliyekuwa mkuu wa Jeshi la Absalomu ila sasa alikuwa upande wa Daudi. Akaona kwenye jeshi lake amfuate Sheba maana ataleta shida kupita Absalomu. Yoabu naye akaenda na alipomkuta Amasa akamwambia kwa unafiki "amani kwako ndugu yangu" kisha akamshika Amasa ndevu kwa mkono wake wa kuume ili ambusu, naye hakujua kama Yoabu ana upanga mkononi mwake, naye Yoabu akamchoma tumboni, na utumbo ukamwagika chini, akafa. Yoabu na Abishai wakamfuata Sheba, na kumhusuru katika mji wa Abeli wa Bethmaaka. Hapo wakakutana na mwanamke mmoja mwenye akili au tuseme hekima, wakati wakiwa wanataka kubomoa ukuta kumpata Sheba. Mwanamke huyu akasema wamsikilize na wamwite Yoabu ili azungumza naye. Naye Yoabu akaja. Yule mama

akasema yeye ni mtu wa amani na mwaminifu katika Israeli, nao watafuta kuharibu mji, na kuumeza urithi wa BWANA. Yoabu akamwambia yule mama ampe ushauri ili asimeze urithi wa BWANA, naye akasema kuhusu Sheba ambaye ameinua mkono wake juu ya ufalme, atawaambia watu wa mjini wamtoe, ili asiwaletee matatizo bure. Yule mwanamke akamwambia Yoabu angoje nje ya mji naye atatupiwa kichwa cha Sheba juu ya ukuta. Akaenda kwa watu wa mji, na kwa akili akawaambia la kufanya, nao wakamkata kichwa Sheba, mwana wa Bikiri na kumtupia Yoabu nje. Tarumbeta ya ushindi ilipigwa na watu wakatawanyika toka mjini kila mtu kwenda hemani mwake, na Yoabu akarudi mpaka Yerusalemu kwa mfalme.

Yoabu alikuwa juu ya jeshi lote la Israeli, Benaya juu ya Wakerethi na Wapelethi, Adoramu juu ya shokoa, Yehoshafati juu ya kumbukumbu, Shausha alikuwa mwandishi, Sadoki na Abiathari makuhani na Ira kuhani wa mfalme Daudi. Kulikuwa na njaa siku za Daudi miaka mitatu, na alipoutafuta uso wa BWANA akaambiwa ni kwa sababu nyumba ya Sauli ilimwaga damu, kwa kuwaua Wagibeoni. Mfalme aliwaita Wagibeoni na kuuliza, afanye nini ili kuondoa hiyo ghadhabu? Akawaambia waseme lolote. Wagibeoni walisema hawataki fedha au dhahabu ila watundikwe watu saba wa familia ya Sauli maana aliwaharibu wasikae katika mipaka yoyote ya Israeli. Uovu wa mfalme Sauli ulimfanya mfalme Daudi akamwacha Mefiboshethi kwa ajili ya kiapo chake na Yonathani ila akawatwaa wana wawili wa Rispa suria wa Sauli, na wana watano wa Merabu binti Sauli, nao wakatundikwa na kuangamia siku za mavuno ya shayiri. Naye Rispa akaomboleza wanawe akivaa magunia na akatandika matandiko mlimani tangu mwanzo wa mavuno mpaka mvua ikanyesha akifukuza ndege. Rispa alikuwa na uaminifu wa ajabu. Maana ya jina lake ni 'makaa yanayowaka' alikuwa pale kwa uaminifu, akiwaka. Ujasiri wa Rispa usiku na mchana ukamkumbusha Daudi kutwaa mifupa ya Sauli na Yonathani kutoka Yabeshi-gileadi na kuizika, kisha Mungu akaridhia nchi na njaa ikaondoka.

Kisa cha Rispa ni cha mtu asiyehusika na uovu moja kwa moja, ila uzao wake ukahusika na hivyo ikawa huzuni kubwa sana kwake. Rispa yupo kwenye ukingo wa kisa cha Mfalme Daudi na anatupa mafundisho fulani. Akiwa suria wa mfalme wa awali, alikuwa na machache ya kufanya kama inavyoonekana. Kwa kweli, hatima yake ilionekana kuwa mbaya na ya kutisha. Wanawe wawili wakiwa wamekufa, familia kubwa zaidi ya "mume" wake aliyekufa ikikaribia kuangamizwa, hata hivyo yeye alitenda kwa uungwana, badala ya kuketi kwenye kona na kuomboleza bahati yake mbaya. Uwepo wake katika nyakati mbili muhimu za historia ya Daudi unamfanya kuwa mjenzi wa taifa. Sote tunaweza kujifunza kitu muhimu sana kutoka kwa Rispa: uaminifu hautegemei hali au bahati nzuri (au mbaya). Uaminifu ni ahadi isiyo na masharti ya kufanya yaliyo sawa bila kujali gharama na huku tukimtegemea Mungu kwa ushauri. Injili ni ujumbe wa amani. Injili ni ujumbe wa amani. Ukristo ni mfumo ambao, ukipokelewa na kutiiwa, ungeeneza amani, maelewano, na furaha duniani kote. Dini ya Kristo itaunganisha wote wanaokubali mafundisho yake. Ilikuwa kazi ya Yesu kuwapatanisha wanadamu na Mungu, na hivyo wao kwa wao

Kulikuwa na vita na Wafilisti tena Gobu, Daudi akaenda vitani na kuishiwa nguvu, na Mrefai aliyeitwa Ishi-benobu akaja amejifunga upanga tayari kumwua Daudi,

ndipo Abishai akamsaidia na kumpiga huyu Mfilisti na kumwua. Watu wa Daudi wakamwambia, “hutatoka tena pamoja nasi kwenda vitani, usije ukaizima taa ya Israeli.” Basi waliendelea kupigana na Wafilisti kutoka Gathi, kule kwa Goliathi, na kupata ushindi.

*Wagonjwa wataongozwa kwa Kristo kwa uangalifu wa wauguzi ambao wanayawazia mahitaji yao, na ambao huinama katika ombi na kumwomba Mmishonari Mkuu wa Tiba kumtazama kwa huruma mgonjwa anayeteseka na kuruhusu ushawishi unaotuliza wa neema Yake usikike na urejesho wa nguvu Zake udhihirike.

---

Wagibeoni waliridhishwaje? Unajifunza nini kutoka kwa Rispa? Kwa nini Abishai alimwua Mfilisti? Barzilai alikuwa ni nani? Kwa nini Yoabu alimwua Amasa?

**SIKU YA 100**
**(Aprili 9)**

# Mashujaa wa Daudi

**- 2 Samweli 22-23**



Basi Daudi akaimba wimbo, siku ile Bwana alipomwokoa mikononi mwa adui zake wote, na mkononi mwa Sauli.

"Bwana Ndiye jabali langu, na Ngome yangu, na Mwokozi wangu, naam, Mungu wa Mwamba wangu, nitamwamini Yeye; ngao yangu, na pembe ya wokovu wangu, mnara wangu, na makimbilio yangu; Mwokozi wangu, Aniokoa na jeuri. Nitamwita BWANA astahiliye kusifiwa; hivyo nitakokoka na adui zangu. Maana mawimbi ya mauti yalinizunguka, Mafuriko ya uovu yakanitia hofu. Kamba za kuzimu zilinizunguka; Mitego ya mauti ilinikabili. Katika shida yangu nalimwita BWANA, nami nikamlalamikia Mungu wangu. Naye akasikia sauti yangu hekaluni mwake, kilio changu kikaingia masikioni Mwake… Akanishika; akanitoa katika maji mengi; Akaniokoa na adui yangu mwenye nguvu, Na wale walionichukia, Maana walikuwa na nguvu kuliko mimi… BWANA alikuwa tegemeo langu… Kwa kuwa Wewe U taa yangu Ee Bwana; Na BWANA Ataniangazia giza langu. Maana kwa msaada wako nafuatia jeshi; kwa msaada wa Mungu wangu naruka ukuta. Maana ni nani Aliye Mungu ila BWANA? Ni nani Aliye Mwamba, ila Mungu wetu? Mungu Ndiye Ngome yangu yenye nguvu, Naye huwaongoza wakamilifu katika njia Yake…. Umenifunga mshipi wa vita… Adui zangu umewafanya wanipe kisogo… Umeniokoa na mashindano ya watu wangu; Umenihifadhi niwe kichwa cha mataifa; watu nisiowajua watanitumikia. Wageni watanijia wakinyenyekea kwa kusikia habari yangu…Na atukuzwe Mungu wa Mwamba wa wokovu wangu…. Anipatiaye Kisasi na kuwatweza watu chini yangu… Nitakushukuru kati ya mataifa, Nami nitaliimbia Jina Lako. Ampa mfalme Wake wokovu mkuu…… Umefanya nami Agano la milele."

Hizo ndizo zilikuwa nyimbo za mwisho mwisho za Daudi mwana wa Yese, mtungaji wa nyimbo za Israeli mwenye kupendeza, hata leo nawe upatapo shida imba hizi Zaburi za mfalme Daudi.

Basi ufalme wa Daudi uliorodhesha mashujaa thelathini na saba wa vita. Kisha kati ya hao walichuja tena na wakapata watatu ambao ni mashujaa bora zaidi kati ya wale thelathini. Wa kwanza anayeorodheswa ni Yashobeamu mkuu wa maakida aliyeliinua shoka juu ya watu mia nane waliouawa pamoja. Kikosi cha Wafilisti

kilikuwa karibu nao kwenye ngome katika bonde la Warefai. Daudi akawa na kiu na kutamani maji akasema, “Laiti mtu angeninywesha maji ya kisima cha Bethlehemu, kilicho karibu na lango.” Basi hao mashujaa watatu wakapenya na kuteka maji toka kisima kile na kumletea Daudi. Daudi aliyamimina haya maji kama sadaka, hakukubali kuyanywa akisema, “Hasha, BWANA nisifanye hivi; Je! Si damu hii ya watu hao waliohatarisha nafsi zao?” Hayo ndiyo waliyofanya wale mashujaa watatu. Abishai ndugu wa Yoabu alikuwa mmoja wapo wa mashujaa watatu, aliua watu mia tatu kwa mkuki wake. Naye Benaya aliua simba wawili wakali wa Moabu, na katika shimo la theluji, naye akawa mlinzi wa Daudi. Asaheli naye alikuwa mmoja wapo wa wale thelathini, na hata Uria Mhiti aliyekuwa mume wake Bath-sheba.

BWANA Ndiye atufanyaye mashujaa, tukimtumaini, na kumtegemea, atatufanyia makuu na kutusimamisha hata katika siku ya taabu yetu, atatupa ujasiri mkubwa. Ushujaa wa leo si kuua simba au kuua watu, bali ni kuwa na tabia ya Mungu, kusaidia watu wenye shida na dhiki, kusoma Neno la Mungu kila siku na kuomba, na kutubu dhambi zetu. Huo ndio ushujaa wa leo, yaani kumcha Mungu na kumtukuza kwani saa ya hukumu Yake imekaribia sana, kuichukia dhambi na kwenda kuwaonya wengine pia, kuhusu ujio wa Masihi wa hivi karibuni!

Basi pale hukupata fursa ya kufanya ushujaa kwenye kazi ya Mungu, na ungetaka kufanya kitu kikubwa, Mungu anajua moyo na nia yako ya kufanya mambo mengi kwa ajili Yake. Usivunjike moyo ikiwa kwa majaliwa yake hupati kutimiza mipango hiyo mizuri kwa utukufu Wake. Anakubali matamanio yako na kumwaga baraka Zake, Yeye Anakujua. Amekuvusha katika mambo mengi na anaona uwezo wako hata kabla hujaanza kupanga mipango ya kulitukuza Jina Lake. Anaridhika na moyo wako tu, ndio, moyo wako unaompenda na uliopondeka. Hiyo ndiyo tu zawadi Anayotaka. Kisha unaweza kuendelea kumpelekea mawazo hayo au mengine uliyovuviwa Kwake na kusikia kile Anachosema. Atajipatia Utukufu kupitia wewe.

Tunaishi katika ulimwengu ambao tunahitaji kuwa mashujaa, maana Shetani ni kama simba angurumaye akitafuta ni nani ammeze. Japo tu wadhaifu, ila tukiwa magotini na kujazwa na Maneno Yake Bwana mioyoni mwetu, tutakuwa mashujaa na watu wa pekee.

*Wauguzi wa kimishonari wanapowajali wagonjwa na kupunguza shida za maskini, watapata fursa nyingi za kuomba pamoja nao, kuwasomea Neno la MUNGU, kuzungumza juu ya Mwokozi .... Wanaweza kuleta mwanga wa tumaini katika maisha ya walioshindwa na waliokata tamaa.

---

Soma maneno machache ya Zaburi ya Daudi kwenye kesha la leo? Mashujaa watatu walifanya jambo gani pamoja? Ufalme wa Daudi ulikuwaje wa milele? Tunawezaje kuwa mashujaa leo?

**SIKU YA 101**
**(Aprili 10)**

# Daudi Awahesabu Israeli

**- 2 Samweli 24 na 1 Mambo ya Nyakati 21**

Daudi alimkasirisha Bwana kwa kuhesabu watu. Shetani alimwingia na akamwita Yoabu na kumwambia aende akahesabu Israeli na Yuda. Hata naye Yoabu aliyekuwa na shida za kiroho nyingi, na ukatili pia, aliona hili ni makosa. Akamwambia azunguke katika makabila yote "apate kujua jumla ya watu hao." Hii haikuwa sensa ya kawaida, maana tunaona watu wamehesabiwa kuanzia watoke Misri, na hata kuna kitabu cha Hesabu cha kuhesabu watu. Yoabu kwa hekima akasema, "BWANA, Mungu wako na awaongeze watu hesabu yao ikiwa yoyote mara mia, tena macho ya bwana wangu mfalme na yawaone; ila kwa nini neno hili limempendeza bwana wangu mfalme?" Yoabu akaongeza "kwa nini awe na sababu ya hatia katika Israeli?" Lakini neno la mfalme likawa na nguvu juu ya Yoabu na juu ya majemedari wa jeshi, naye akatoka na majemedari wa jeshi machoni pa mfalme na kwenda kuwahesabu watu wa Israeli. Wakavuka Yordani wakafanya sensa wakienda makabila yote hata mipakani, ikawachukua miezi tisa na siku ishirini. Siku zile ambazo teknolojia ilikuwa ndogo, ilichukua muda kuhesabu watu, kwa mwendo wa mguu na nyumba kwa nyumba. Mfalme alitaka watu wahesabiwe wa umri wa kuwa jeshini, ili ajivunie kwamba jeshi lake ndilo kubwa na pengine anashinda kwa sababu ya maarifa, teknolojia au jeshi lake kubwa. Yoabu akamwambia watu ambao ni zaidi ya miaka 20 ambao wanaweza kusajili jeshi ni 800,000 katika Israeli na 500,000 katika Yuda. Ila hawakuhesabu Walawi na Benjamini kwani hakuafikiana na wazo la mfalme. Hapa Yoabu alikuwa sawa. Je ni mara ngapi nasi tungependa watu wa kanisa letu au kikundi chetu wawe namba kubwa ili tujigambe kwa namna fulani baada ya kuijua hiyo namba?



Basi moyo wake Daudi ukamchoma baada ya kuwahesabu Israeli, naye Daudi akaungama kwa BWANA kwamba amekosa sana kwa aliyofanya. Akasema, "nakusihi uuondolee mbali uovu wa mtumishi wako; kwani nimefanya upumbavu kabisa." Inaonekana alikiuka masharti yaliyo wazi kabisa kutoka kwa Mungu. Daudi alipoamka asubuhi, Gadi, nabii, alimjia akiwa ametumwa na Mungu kwamba achague adhabu moja kati ya tatu. Ya kwanza, miaka saba ya njaa ije nchini, ya pili, miezi mitatu akimbie mbele ya adui zake huku wakimfuatia, au achague siku tatu iwe tauni katika nchi. Akamwambia mfalme afanye shauri, afikiri papo hapo,

ili amrudishie jibu “Yeye aliyemtuma.” Daudi akaingia mashaka sana, na kusema “sasa na tuanguke katika mkono wa BWANA kwa kuwa rehema zake ni nyingi; wala nisianguke katika mkono wa wanadamu.” Basi BWANA alileta tauni toka asubuhi mpaka jioni, na wakafa watu 70,000, ila malaika aliponyosha mkono wake kuelekea Yerusalemu ili auharibu, BWANA akaghairi katika mabaya, na kumwambia yule malaika “yatosha sasa ulegeze mkono wako.” Naye yule malaika wa BWANA alikuwako karibu na kiwanja cha kupuria cha Arauna Myebusi. Daudi alipomwona malaika aliyepiga watu, akaanguka kifudifudi na kusema, kwamba ni yeye mfalme aliyekosa na kupotoka, “Lakini kondoo hawa, wamefanya nini? Mkono wako na uwe juu yangu, na juu ya nyumba ya baba yangu.” Basi Gadi nabii akaenda kwa Daudi akamwambia akwee na kumwinulia BWANA madhabahu penye kiwanja cha Arauna, Myebusi. Daudi akakwea huko kama BWANA alivyoamuru, na Arauna alipomwona mfalme, alitoka na kusujudu kwa mfalme kifudifudi hata nchi na kusema, “bwana wangu mfalme amenijia mtumwa wake kwa kusudi gani.” Naye Daudi akasema makusudi yake, ni kununua kiwanja chake ili amjengee BWANA madhabahu, ili kwamba adhabu ya tauni pate kuzuiliwa katika watu.

Arauna akamwambia akichukue tu, “akatolee yaliyo mema machoni pake”. Kisha akampa mfalme ng’ombe wa sadaka ya kuteketezwa, vyombo vya kupuria, kuni, na vitu vyote akisema, “Ee mfalme, mimi Arauna nakupa wewe mfalme, … Bwana Mungu wako na akukubali. Lakini mfalme akamwambia Arauna, la sivyo, sitachukua kwako bure bali nitavinunua vitu hivi kwako kwa thamani yake; sitamtoelea BWANA, Mungu wangu, sadaka za kuteketezwa zisizonigharimu.” Daudi akakinunua kiwanja cha kupuria na wale ng’ombe kwa shekeli hamsini za fedha na shekeli 600 za dhahabu kwa uzani; naye akamjengea BWANA madhabahu huko, akatoa sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani, na BWANA akaikubali sadaka yake, akaibariki nchi na tauni ikazuiliwa katika Israeli.

Daudi alikubali dhana ya kidunia ya mafanikio; ufanisi ulipimwa kwa ukubwa wa jeshi. Kiburi na tamaa mbaya ndiyo iliyomchochea mfalme kuchukua hatua hiyo. Ukuu wa Israeli kama watu wa Mungu haukuja kutokana na ukubwa wa jeshi lake, au utisho wake kwa mataifa. Ukuu wao ulipatikana katika utii wao kwa Mungu wao, na Mungu aliwafanya kuwa kichwa na si mkia, kwani Mungu alikuwa ameahidi, akisema: Itakuwa utakaposikia sauti ya Bwana, Mungu wako, kwa bidii, kutunza kuyafanya maagizo yake yote nikuagizayo leo, ndipo Bwana, Mungu wako, atakapokutukuza juu ya mataifa yote ya duniani; na baraka hizi zote zitakujilia na kukupata usikiapo sauti ya Bwana, Mungu wako. Utabarikiwa mjini, utabarikiwa na mashambani. Utabarikiwa uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, maongeo ya ng’ombe wako, na wadogo wa kondoo zako. Litabarikiwa kapu lako, na chombo chako cha kukandia unga (Kumb 28).Ilikuwa ni katika kutimiza ahadi hii kwamba Mungu alikuwa amepigana na kushinda kwa niaba ya Israeli katika vita vyote walivyopigana. Sio ukubwa wa jeshi lao ndiyo ulishinda vita. Kupima mafanikio kwa njia ya ulimwengu kulimfanya Daudi atende dhambi nzito.

*Ikiwa maombi zaidi yangetolewa katika vyumba vyetu vya Sanitarium vya wagonjwa wa muda mrefu kwa ajili ya uponyaji wa wagonjwa, nguvu kuu ya Mponyaji

ingeonekana. Wengine wengi wangeimarishwa na kubarikiwa, na magonjwa mengi ya dharura (papo hapo) yangeponywa.

---

Nabii Gadi alimwambiaje Daudi? Kwanini si vizuri kujigamba kamba mna washiriki wengi? Mungu anapenda hesabu hata ana kitabu cha Hesabu, kwanini alichukizwa na wazo la Daudi? Daudi alichagua adhabu gani? Daudi alimwambia nini Arauna? Kwa nini sadaka wanazotupatia watu kutoa tukiwa na zetu, ni wao wametoa na wala si sisi?

**SIKU YA 102**
**(Aprili 11)**

# Kutawazwa kwa Sulemani

**- 1 Wafalme 1**



Daudi alinuia siku za uzee wake kuweka hazina ya kujenga hekalu la Mungu juu ya mlima Moria, huu ndio mlima ambao Ibrahimu alikwenda ili kumtoa mwana wake Isaka kama sadaka. Hekalu lingekuwa jengo lenye thamani kubwa kupita yote. Daudi alitaka kufanya kazi hii lakini Bwana alimwambia, amekuwa mtu wa vita na kumwaga damu, na nyumba yake itajengwa na mtu wa amani.

Daudi akapata baridi kwa uzee, wakamfunika nguo, isisaidie. Basi alitafutiwa Abishagi, mshunami akamtunza mfalme na kumtumikia. Habari hizi zimeandikwa kwa ufupi, na japo Daudi alikuwa na wengi wa kumtunza Abishagi aliletwa, mengine yanayoandikwa kwenye Biblia si kwamba Mungu ameyaagiza, ila ameruhusu au pengine hakuyazuia, na yanawezekana yakawa ni mpango wa mwanadamu au mpango wake. Haya ni yale tutayuliza mbinguni, tuombeane tuwe kule!

Adonia, aliyekuwa kijana wa Daudi mkubwa baada ya Amnoni na Absalomu kufa, akafikiri kama desturi ndiye atakuwa mfalme. Akajiwekea tayari magari na wapanda farasi 50 wapige mbio mbele yake kama Absalomu, na babaye hakumchukiza wakati wowote. Akashauriana na Yoabu jinsi watakavyomiliki, na Abiathari kuhani. Ila Sadoki kuhani na Benaya, Nathani na Shimei mashujaa wa Daudi hawakuwa pamoja na Adonia. Adonia akachinja vinono kwa watu na kuwaita ndugu zake au wana wa mfalme na watu wa Yuda, ila hakuwaita Nathani nabii, Benaya, mashujaa au Sulemani nduguye. Nathani akamwambia Bath-sheba mamaye

Sulemani aliyeahidiwa ufalme na baba yake, kwamba Adonia anamiliki na Daudi hana habari. Akampa ushauri aende kwa Daudi ili aokoe roho yake na Sulemani, na amwambie kwamba alimwapia, "kusema hakika yake Sulemani mwana wako atamiliki baada yangu." Basi Bath-sheba akaenda na kueleza kwa mfalme Daudi, akasema hoja yake, na kwamba Adonia amechinja vinono, na Yoabu na Abiathari wamemfuata, ila Sulemani hakuitwa. Akamwambia Israeli wote wanangoja aseme ni nani mrithi wake, maana atakapokufa watapata shida na mwanawe Sulemani. Alipomaliza kusema Nathani nabii akaingia na kusujudu kifudifudi kwa mfalme na kuthibitisha yale maneno yaliyosemwa na mama yake Sulemani. Basi Mfalme akaagiza Bath-sheba aitwe, naye akaapa akisema "BWANA aishivyo, aliyenikomboa roho yangu katika shida zote … Sulemani mwanao atamiliki baada yangu, naye ndiye atakayeketi katika kiti changu cha enzi…" Bath-sheba akainama kifudifudi akamsujudia mfalme na kusema "Bwana wangu aishi milele." Mfalme akamwita Sadoki kuhani, Nathani nabii na Benaya, wakaja, naye akawaambia watwae watumishi wa mfalme, wamtwae Sulemani na kumpandisha juu ya nyumbu wake mwenyewe na waende mpaka Gihoni, kisha Sadoki kuhani na Nathani nabii wamtawaze kwa kumtia mafuta awe mfalme wa Israeli. Kisha wapige na tarumbeta wakisema, "Mfalme Sulemani na aishi… Kwa maana atakuwa mfalme badala yangu; ndiye niliyemweka awamiliki Israeli na Yuda." Benaya akasema, enzi ya Sulemani na iwe "tukufu kuliko kiti cha enzi cha bwana wangu mfalme Daudi." Wakashuka hao na kumtawaza Sulemani, na kupiga panda, wakafurahi mno, hata nchi ikavuma kwa sauti zao. Adonia, Yoabu na wageni waliposikia sauti hizo walipokuwa wakila vinono waliacha karamu yao na kutaharuki. Basi Yonathani akafika, naye akasema yaliyotokea, kwamba Sulemani ametawazwa na Sadoki, Nathani na Benaya wako upande wake. Kisha amepandishwa juu ya nyumbu wa mfalme na Wakerethi na Wapelethi, wametoka wakifurahi, na ndiyo kelele wanazosikia. Sulemani ameketi katika kiti cha enzi cha ufalme na watumishi wa mfalme wanambariki wakisema Mungu akuze jina la Sulemani kuliko la Daudi na kukifanya kiti chake cha enzi kiwe kitukufu kuliko kiti chake. Mfalme Daudi akafurahi kwamba BWANA amempa urithi wa mtu kukaa katika kiti chake, macho yake yakiwa yanaona bado.

Adonia na wageni wake wakaogopa na wakatawanyika, Adonia akenda madhabahuni na kushika pembe zake ili kujisalimisha. Sulemani akasema kama ni mtu wa kweli, hata unywele mmoja wake hautaanguka chini, lakini uovu ukionekana ndani yake atakufa. Akatuma watu wamtelemshe toka madhabahuni. Adonia akaenda kwa Sulemani na kumwinamia, naye Sulemani akamwambia aende nyumbani kwake. Mama za watoto wa Daudi waadilifu, pengine ndio walichangia ushawishi chanya kwa watoto wao kuliko mfalme aliyeshugulika na taifa zima. Moyo wangu unawaendea wanaume walio na shughuli nyingi za kuongoza makanisa au serikali. Yapaswa tuwaombee wao, na watoto wao, na kujiombea wenyewe na watoto wetu. Je, umemwuliza Mungu kuhusu nafasi ambayo unataka kuitwaa, kabla hujaingia kwenye huo wadhifa? Adonia alipaswa kufanya hivyo.

Daudi alitoa wosia na urithi wake alipokuwa bado hai, Kutoa vitu vyako baada ya kufa, si kutoa maana unavishikilia kwa uchoyo ukifikiri unavihitaji, nawe unajua huwezi kwenda navyo kokote. Kaburini na wala mbinguni hatutakwenda na vitu huko, tafuta jinsi ya kusaidia masikini, yatima, na wajane hapa duniani ukiwa hai

bado. Sisi ni mawakili na wasimamizi wa yale ambayo Mungu ametukabidhi; Yeye ni mmiliki wa vyote, na Yeye Ndiye anayetupa uzima. Katika kutoa kwa kazi ya Mungu, tunajiwekea hazina mbinguni. Yote unayoyaweka juu mbinguni ni salama na huongezeka hadi kuwa ya milele, na ya kudumu. Kuna faida nyingi za kutoa sasa, wakati bado tuna pumzi ya uhai.

Hapa kuna machache:

1. Utaona matokeo ya zawadi zako—jengo jipya la kanisa, kijana chuoni, na yatima mwenye furaha
2. Hakuna malumbano kati ya familia au marafiki baada ya kifo chako.
3. Mfano mzuri wa maadili ya familia ya ukarimu na upendo kwa wengine.
4. Inaonyesha kwamba moyo wa mtoaji umebadilishwa kutoka kwenye ubinafsi na kuelekea ukarimu
5. Huweka hazina mbinguni.

*Ningeenda mbele za Bwana na ombi hili: "Bwana, hatuwezi kusoma moyo wa mgonjwa huyu, lakini unajua huenda ni kwa faida ya roho yake na kwa utukufu wa Jina Lako kumuinua kiafya. Kwa wema Wako mkubwa, ulirehemu jambo hili (mhurumie mgonjwa), na ruhusu hatua za kiafya zifanyike katika mfumo. Kazi lazima iwe Yako Mwenyewe kabisa. "

---

Kwa nini Daudi alimweka Sulemani awe mfalme kabla hajafa? Abishagi mshunami alitafutwa kwa ajili gani kwa mfalme uzeeni? Nathani alimpa ushauri gani Bath-sheba? Ni watu gani walikuwa upande wa Adonia? Unafikiri kwanini Daudi alichoka au kuzeeka sana akiwa na miaka 70 tu?

**SIKU YA 103**
**(Aprili 12)**

# Zaburi - Nyimbo na Ibada

**- Zaburi 1-150**




Zaburi ndiyo kitabu kirefu kupita vyote vya Biblia. Ina sura 150. Zaburi 119 ndiyo sura refu kupita zote katika Biblia na Zaburi 118 ndiyo iliyo katikati ya Biblia. Sura ya 117 ya Zaburi ndiyo sura fupi kupita zote katika Biblia. Kitabu cha Zaburi ni nyimbo na kitabu cha maombi. Waandishi mbalimbali waliandika kama vile Daudi, Asafu, Musa, Sulemani, nk. Daudi ndiye mtunzi mkuu au ndiye mwenye mashairi mengi katika Zaburi. Nyimbo na maombi haya yalikusanywa na wana Israeli kwa ajili ya ibada, na ni sehemu ya Maandiko Matakatifu. Daudi alisema, "Nitamwimbia BWANA maadamu ninaishi, nitamshangilia Mungu wangu nikiwa hai!" Zaburi 104:33. Watu wa kwanza kuandika Zaburi ni kama Musa, aliyeandika Zaburi ya 90 akikumbusha kwamba tunaishi muda mfupi tu wa miaka sabini au themanini. Basi akamwomba Mungu atufundishe "kuzihesabu siku zetu, tujipatie moyo wa hekima, maana zinapita haraka." Hivyo tumtii na kumtegemea Mungu kabla hatujalala usingizi wa mauti.

Zaburi ni aina ya mashairi, na kila lugha ina kanuni zake za mashairi. Mashairi ya Kiswahili, yana beti nne, na beti ya nne hurudia, na vina ni maneno manane. Mashairi ya kingereza haijalishi kuhesabu maneno, bali yawe yana sauti inayofanana mwishoni. Mashairi ya Kiebrania, sentensi ilirudiwa na kutiliwa mkazo.
Mfano mzuri ni mlinganisho wa mtu mwovu na mwema wa Zaburi moja: Zaburi 1
"Heri mtu asiyekwenda katika shauri la wasio haki; Wala hakusimama katika njia ya wakosaji; Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha.

Bali sheria ya BWANA ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na

usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji.
Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki,
Na kila alitendalo litafanikiwa."

Unaona uovu au wema, waendelea ukiota mizizi au ukikua. Mfano: kwanza kwa kwenda kwa watu waovu, kisha kusimama, kisha kukaa, pengine hata kulala, na ndiyo anazama kabisa katika uovu.

Mashairi ya Zaburi ni ya aina nyingi, mfano mashairi ya kumsifu Mungu, kumwadubu Mungu, kumwomba Mungu msaada, kuomba ulinzi na wokovu, kuomba msamaha, kutoa shukurani kwa baraka za Mungu, kuomba maadui wetu washughulikiwe. Maombi ya Zaburi ni ya mtu binafsi, na wakati huo huo ni ya taifa zima. Mengi yanaonesha mahusiano ya karibu na muhimu mno kati ya Mungu na watu. Na mengine yanawakilisha mahitaji na hisia za watu wote wa Mungu.

Zaburi imenukuliwa mahali pengi kwenye agano jipya, ukisoma tu utajua ni mtindo wa Zaburi. Mfano wimbo wa Mariamu wa Luka 1:46-55, unabii wa Zakaria wa Luka 1:68-79 au ombi la Shukurani la mcha Mungu Simeoni katika Luka 2:29-32. Zaburi ina unabii mwingi wa Masihi. Yesu alinukuu Zaburi na hata waandishi wa Biblia wameinukuu. Kitabu hiki ni tunu ya ibada kwa waumini toka zamani na hata leo. Kuna uzuri wa ajabu katika kitabu hiki. Soma Zaburi na uzifurahie. Nimeipenda Zaburi 119, inatuonesha kwa kina amri, maagizo, sheria, shuhuda, na mausia ya Mungu. Hebu tuseme pamoja na Daudi, "Ningependa njia zangu ziwe thabiti, Nizitii amri Zako. Ndipo mimi sitaaibika, Nikiyaangalia maagizo Yako." Zaburi 119:5-6.

Zaburi 23, 37, 40, 77 na 140 zimekuwa msaada kwangu wakati nikiwa na shida. Na bila shaka Zaburi 23 ndiyo inayopendwa kupita zote kwa kukaririwa. Daudi anatuonesha wazi kwa kusema hatuna haja ya kuogopa. "BWANA ni nuru yangu na wokovu wangu, nimwogope nani? Kweli Yeye ni ngome ya uzima, hatuna haja ya kuhofu. Hebu nafsi zetu zisisahau fadhila Zake, tuinue macho yetu na kuona msaada wetu unatoka Kwake. Kila mtoto na mtu mzima angekariri hii, kama vile tunavyokariri sala ya BWANA. Naiweka hapa ili ujipe wiki ya kuikariri, maana tupatapo shida, msaada wetu utatoka kwa Mungu. Wengine wanaweza kupenda kutusaidia, ila mara nyingine pia wanashindwa, hivyo tujifunze kumwita Mungu na kumlilia katika shida zetu.

Zaburi 23
"Bwana ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu.
Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, Kando ya maji ya utulivu huniongoza.
Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza, Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.
Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya; kwa maana Wewe upo pamoja nami. Gongo Lako na fimbo Yako vyanifariji,
Waandaa meza mbele yangu, Machoni pa watesi wangu, Umenipaka mafuta kichwani pangu, Na kikombe changu kinafurika,
Hakika wema na fadhili zinanifuata siku zote za maisha yangu; Nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele."

Zaburi inatupatia matumaini kwamba japo sisi ni kama maua yanayonyauka au moshi unaopita, bado Mungu anatujali mno. Daudi alishangaa ukuu wa Mungu na kusema katika Zaburi 19, "Mbingu za uhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono Yake." "Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole Vyako, mwezi na nyota ulizoziumba, mtu ni kitu gani hata umkumbuke? Na Binadamu hata umwangalie?"

Daudi aliuliza maswali ambayo hata leo tunajiuliza, mfano, "BWANA, kwa nini unanyamaza kimya wakati wa shida yangu." Mara zingine aliona kama watu waovu ndio wanafanikiwa na kuwa matajiri, ila wengine wanapata maumivu na shida, japo wanamwabudu na kumpenda Mungu. Katika Zaburi 77 akasema yale yaliyokuwa moyoni mwake, kwamba alikuwa karibu kukata tamaa kwani watu waovu, matajiri na wenye kiburi ndiyo wananeemeka. Anasema mpaka alipoenda hekaluni na kuona hukumu yao ya mwisho, ndipo alijua kwamba mwisho wao si mwema, hivyo akaacha kuwaonea wivu, au kupotosha haki ya Mungu.

Zaburi 110 imenukuliwa mara 33 kwenye agano jipya. Fungu ambalo limenukuliwa ni "Neno la BWANA kwa Bwana wangu, uketi mkono wangu wa kuume, hata niwafanyapo adui zako kuwa chini ya miguu yako." Fungu hili linaonesha kuwa Yesu amekaa mkono wa kuume wa Mungu Baba.

Katika Zaburi 139 Daudi anatuambia kuwa BWANA anatujua na anatuchunguza. Njia zetu zote, anazijua, tunapokaa, tunapoinuka na mambo yetu yote, maarifa hayo ya BWANA ni ya ajabu sana. Alijua hawezi kwenda kokote ambako Mungu hatapafahamu, akienda mbinguni Yeye yupo, akija duniani yupo, hata giza halimfichi Mungu kitu. Anasema, "Wewe ndiwe uliyeniumba toka chembe ndogo nilipokuwa kwenye tumbo la mama yangu, uliniunga tumboni. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu ya kutisha, matendo yako ni ya ajabu ... Macho yako yaliniona tumboni mwa mama yangu kabla sijakamilika, nilipoumbwa kwa siri, nilipoungwa kwa ustadi." Mtunga Zaburi anamwomba Mungu amchunguze ili ajue kama kuna njia yake yoyote inayoleta majuto, ili aungame na kuwa na furaha katika maisha yake.

Zaburi 150, ni Zaburi ya kumsifu Mungu na inamalizia kwa kutukazia tumsifu BWANA katika Patakatifu Pake kwa matendo Yake makuu na tutumie baragumu, kinanda, matari, kinubi, zeze, filimbi, matoazi, na zaidi kila mtu, "Kila mwenye pumzi na amsifu BWANA. Haleluya!" Bwana huishi katika sifa za watu Wake, hakuna kitu chema kama kumsifu BWANA. Kwani yeye ana kila kitu, tutamrudishia nini kwa mema, baraka anazotufanyia kila siku kama si kumsifu, kutoa ushuhuda kwa watu wengine ili wamjue. Vyombo vya muziki vikitumiwa ipasavyo, bila ya kuwa na makelele kama ya nyimbo za dunia, ni jambo jema sana, hebu vyombo hivi vitumiwe vyema, na watu waweze kusikia matamshi ya maneno ya wimbo.

Zaburi ina utajiri mwingi. Zaburi 34, "Nitamhimidi Bwana kila wakati, Sifa Zake zi kinywani mwangu daima… Nalimtafuta BWANA akanijibu, akaniponya na hofu zangu zote. Malaika wa BWANA hufanya kituo akiwazungukia wamchao na kuwaokoa. Onjeni na mwone ya kuwa BWANA Yu mwema." Hata leo nakusisitizia

uonje, na kujua kuwa BWANA yu mwema.

Katika Zaburi zote mimi naipenda ile ya 119 zaidi, ambayo ni mashairi nane, yenye beti nane nane, na hivyo ina mafungu 176, yaani 8x22. Kila fungu isipokuwa moja anazungumza kuhusu Neno la Mungu. Tafuta hilo fungu! Neno la Mungu ni Sheria Yake, Maagizo Yake, Kanuni Yake, Amri Zake, Shuhuda Zake. Soma hii Zaburi mara nyingi, na tunapopitia changamoto na hata wakati wa furaha, tusome Zaburi, kwani ni kitabu kinachoburudisha moyo sana! Nikiwa sijui nisome nini, naenda kwenye Zaburi kwanza! Ameziweka hisia za mwanadamu kwa uwazi napopitia changamoto, na hiyo inaleta kiitikio moyoni mwangu!

*Hebu sauti ya maombi isikike katika taasisi zetu kwa niaba ya wagonjwa ili waweze kujiweka mahali ambapo wanaweza kushirikiana na Yeye ambaye anaweza kuponya mwili na roho pia.


---

Ni nani aliandika kitabu cha Zaburi? Waliandika kwa mtindo gani? Zaburi gani zina unabii wa Masihi? Kariri Zaburi 1, 23 na 91. Ni nini ambacho unakumbuka kuhusu Zaburi 119?

**SIKU YA 104**
**(Aprili 13)**

# Sulemani na Maagizo ya Baba Yake

**- 1 Wafalme 2-3**



Daudi akamhusia Sulemani mwanae akisema "mimi naenda njia ya ulimwengu wote; basi uwe hodari, ujionyeshe kuwa mwanamume; Uyashike mausia ya BWANA, Mungu wako, uende katika njia zake, uzishike sheria Zake, na amri Zake, na hukumu Zake, na shuhuda Zake, sawa sawa na torati ya Musa ilivyoandikwa, … upate kufanikiwa katika kila ufanyalo, na kila utazamako, ili BWANA afanye imara Neno Lake alilonena kupitia Daudi, kwamba ikiwa watoto wake wataenda katika njia ya BWANA kwa moyo wote, na roho yote; basi Daudi asingekosa mtu katika kiti cha enzi cha Israeli. Akamwambia yale mabaya aliyoyafanya Yoabu ya kumwua Abneri, na Amasa bila kuwa na vita nao "wala usiwaachie mvi zao kushuka ahera kwa amani." Akamwambia awatendee wana wa Barzilai Mgileadi mema, na waendelee kukaa mezani pake kwa vile walimsaidia wakati wa kumkimbia Absalomu. Lakini Shimei, aliyemlaani Daudi amwangalie, maana ana hekima "utajua yakupasayo kumtendea, na mvi zake utazishusha ahera pamoja na damu. Basi Daudi akafariki. Sulemani akaanza kutawala, katika kiti cha enzi cha babaye Daudi, na ufalme wake ukawa imara sana. Adonia, kaka yake mkubwa kwa mama mwingine akaja tena kwa Bath-sheba mamaye Sulemani na kusema ufalme ulikuwa wake kwa vile yeye ndiye kijana mkubwa ila mambo yamegeuka, kwa ndugu yake kwa mapenzi ya BWANA. Akamwomba haja moja, na akamsihi asimkataze, naye Bath-sheba akamwambie aseme. Adonia akaomba aozwe Abishagi mshunami, aliyempa baba yake joto, naye mama ya Sulemani aliona haina ubaya, atazungumza na mtoto wake

mfalme Sulemani asijue ni mtego. Mama yake Sulemani alipomwulizia hili Adonia kwa Sulemani, akiwa kwenye kiti chake cha enzi, akamketisha mamaye mkono wa kuume. Mama yake akasema ana haja ndogo asimkataze, naye Sulemani akasema, “omba mama kwa kuwa siwezi kukutaza neno” asijue anachoenda kuombwa. Sulemani aliposikia Adonia anataka kumwoa Abishagi alijua ina maana mbaya. Kwa vile alikuwa kama nembo ya mke kwa Daudi, ni kama alitaka pia apewe ufalme, kwani alikuwa anamrithi mke wa mfalme. Akamwambia mama yake, “umtakie na ufalme pia” Adonia, kwa kuwa yeye ni ndugu yangu mkubwa.

Basi Sulemani akaapa kuwa hatamwacha Adonia kuleta shida katika ufalme na akasema “hakika atauawa leo hivi Adonia.” Mfalme akamtuma Benaya kumwua. Akamwambia Abiathari, kuhani aliyemwasi na kuwa upande wa Adonia, aende shambani kwake, naye angeuawa kama si kumsaidia baba yake kwa kuchukua sanduku la agano wakati akiwa katika shida ya kumkimbia Sauli na utesi wake. Akamtoa Abiathari asiwe kuhani, akitimiza Neno la BWANA kwamba uzao wa Eli hawatakuwa makuhani tena. Habari zikamfikia Yoabu, kwani alimfuata Adonia pia, naye akakimbilia kwenye madhabahu na kushika pembe zake kujisalimisha, hapo ndipo Benaya alipotumwa kumwambia atoke kwenye madhabahu, na akapigwa, mfalme akasema ili “uniondolee mimi na nyumba ya baba yangu damu aliyoimwaga bure.” Naye damu yake ikawa kichwani kwake kwa uovu wa kuua watu wasio na hatia kama Abneri na Amasa. Benaya akawa amiri jeshi badala ya Yoabu na Sadoki akawa kuhani badala ya Abiathari. Mfalme akamwita Shimei ajijengee nyumba Yerusalemu na asitoke wala kuvuka Kidroni, ili asilete ubaya mwingine. Akamwambia akitoka na kuvuka atakufa na damu itakuwa juu ya kichwa chake mwenyewe. Shimei akasema sawa, na akakaa Yerusalemu siku nyingi. Ila baada ya miaka mitatu watumwa wake walitoroka kwenda kwa Akishi naye akaondoka na punda kuwafuata Gathi. Mfalme alipata habari na kutuma ujumbe kwa Shimei aletwe kwa vile mfalme alimwapisha akakubali, bali hakusikia maagizo au kiapo kwa BWANA. Akamkumbusha uovu wa moyoni mwake aliomtendea babaye Daudi, basi akaamuriwa auawe.

Sulemani akafanya urafiki na Farao, akamwoa binti yake na akamleta mji wa Daudi na kumjengea nyumba, mbali kidogo na madhabahu. Inaonekana mwanamke huyu alimpenda Mungu wa Israeli kulinganisha na wake wengine wa Sulemani. Huyu ndiye aliyekuwa mke wake wa kwanza na Sulemani.

Tunaishi wakati wa mwisho ambapo shetani anatafuta nani wa kummeza. Ni lazima tuombeane sisi kwa sisi na kutoa onyo la hatari la kutofunga ndoa na wasioamini. Ni lazima kama Ezra tuwajulishe wenzetu hatari ya kufungiwa nira isivyo sawa. Wengi wanahitaji kujua hatari za kuwa na ubia na watu wa ulimwengu. Ni lazima tuonyeshe hatari ya kujishirikisha na siasa zisizompendeza Mungu. Ni lazima tuwahimize vijana wetu kuchagua Elimu ya Kikristo dhidi ya elimu ya dunia. Kuoa asiyeamini kwa nia ya kumleta kwa Bwana baadaye, ni kupuuza maagizo ya Mungu waziwazi. Ni Mungu anayemwongoa mtu na si mwenzi. Kuoa asiyeamini kunamweka mwamini katika hatari ya kutomcha Mungu. Migogoro ya mara kwa mara hutokea na kuvuruga mahusiano. Watoto wanakabiliwa na mfano mbaya wa mzazi asiyemcha Mungu. Mara nyingi muumini hulazimika kuchagua kati ya

Bwana na mke au mume anayempenda. Na Itamsumbua moyoni kwamba mwenzi wake hawezi kwenda mbinguni.

*Hapo awali tulibarikiwa na taasisi ambazo wagonjwa wangeweza kupata msaada dhidi ya mateso, kwa matibabu ya uadilifu na sala za dhati katika imani kwa MUNGU, tulibeba kesi ambazo zilionekana kukosa matumaini kufanikiwa. Leo Bwana anawaalika wanaoteseka kuwa na imani katika Yeye. Hitaji la mwanadamu ndiyo fursa ya MUNGU kutenda (Man's necessity is God's opportunity).

---

Daudi alitoa mausia gani kwa Sulemani? Adonia alimwomba nini Bath-sheba? Alijibiwaje? Kwa nini Yoabu na Shimei waliuawa? Kwa nini Abiathari hakuuawa? Sulemani alioa mke toka wapi?

**SIKU YA 105**
**(Aprili 14)**

# BWANA Amtokea Sulemani

**- 2 Wafalme 3 na 2 Mambo ya Nyakati 1**



Mungu alikuwa na Sulemani na akamtukuza mno. Ufalme wake ulikuwa mkubwa, akitawala toka Dani mpaka Beersheba, Syria, Moabu, Amoni, mpaka mto Frati. Naye alikuwa na watu wengi kama maakida, waamuzi na mashehe anaowaongoza. Mfalme Sulemani akaenda Gibeoni kutoa kafara mahali pa juu. Akatoa sadaka elfu za kuteketezwa juu ya madhabahu ile ya Musa iliyojengwa na Bezaleli na Aholiabu jangwani. Na BWANA akamtokea Gibeoni katika ndoto usiku, na kumwambia, "Omba utakalo nikupe." Sulemani akasema, umemfanyia mtumwa wako Daudi baba yangu fadhili kuu, kadiri alivyoenenda mbele zako katika ile Kweli, haki, na unyofu wa moyo pamoja nawe. Nawe umempa fadhili ya mwana wake kuwa kwenye kiti leo, na kunitawaza kuwa mfalme, badala ya Daudi baba yangu, "Nami ni mtoto mdogo tu, sijui jinsi inipasavyo kutoka wala kuingia. Na mtumwa wako yu katikati ya watu wako uliowachagua, watu wengi wasioweza kuhesabiwa, wala kufahamiwa idadi yao, kwa kuwa ni wengi. Kwa hiyo nipe mimi mtumwa wako moyo wa adili niwahukumu watu wako, na kupambanua mema na mabaya; maana ni nani awezaye kuwahukumu hawa watu wako walio wengi?"

Neno hili likawa jema, machoni pa BWANA ya kuwa Sulemani ameomba hekima, na Mungu akamwambia, kwa vile ameomba neno la kuwatumikia watu na Mungu, wala hakujitakia maisha marefu, mali, utajiri, utukufu, uhai wa adui zako, bali maarifa na akili za kujua kuhukumu; "Tazama nimekupa moyo wa hekima na akili." Kabla yake hapakuwa na mtu mwenye hekima kama yeye na hata baada yake hatainuka mtu kama yeye. Na BWANA akampa yale yote asiyoyaomba kama ziada nyingine, yaani, mali, fahari na maisha marefu akiyashika mausia na maagizo yake kama baba yake. Sulemani aliamka kwenye ndoto hii, na akaenda penye sanduku la agano huko Yerusalemu na kutoa sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani, na kuwafanyia watumishi wake wote karamu.

Sulemani akawa na hekima kupita wanadamu wote. Akazungumza kuhusu

miti, ndege, samaki na wanyama. Ndipo wanawake wawili makahaba, walioishi pamoja, wakaja kwake kutaka kuamuliwa. Kila mmoja alikuwa na mtoto mchanga. Mmoja akasema, "sisi tulikuwa pamoja; hapakuwa na mtu mwingine pamoja nasi nyumbani… Na mtoto wa mwanamke huyu akafa usiku, maana alimlalia. Akaondoka usiku akamwondoa mtoto wangu ubavuni pangu, mimi mjakazi wako nilipokuwa usingizini, akamweka kifuani pake, na mtoto wake mwenyewe, aliyekuwa amekufa, akamweka kifuani pangu. Nilipoondoka asubuhi nimnyonyeshe mtoto wangu, kumbe? Amekufa… Ndipo yule mwanamke wa pili akasema, Sivyo hivyo, bali mtoto wangu ndiye aliye hai, na mtoto wako ndiye aliyekufa, na mwenzake akasema sivyo hivyo; bali mtoto wako ndiye aliyekufa, na mtoto wangu ndiye aliye hai." Wakabishana mbele ya mfalme.

Ndipo mfalme akasema, "Huyu anasema mtoto wangu yu hai, na wako amekufa, na wa pili anasema vile vile, mtoto wangu yu hai wako amekufa." Basi mfalme akaamrisha uletwe upanga. Mfalme akasema, "Mkate mtoto aliye hai vipande viwili, kampe huyu nusu, na huyu nusu." Ndipo yule mwanamke mwenye mtoto aliye hai, akawaza moyoni mwake akimwonea huruma mtoto wake, na hakujali atakayemchukua, iwe yeye au yule mama mwingine. Akamwambia mfalme, "Ee bwana wangu mfalme mpe huyu mtoto aliye hai, wala usimwue kamwe." Ila yule ambaye si mtoto wake alitaka kumwiba tu, alisema, "Asiwe wangu, wala wako, na akatwe." Mfalme kwa hekima aliyopewa na Mungu aligundua ni nani mwenye mtoto na kuamuru, "mpe huyu wa kwanza mtoto aliye hai, maana yeye ndiye mama yake." Israeli wakapata habari za hiyo hukumu aliyotoa mfalme na wakamwogopa mfalme maana waliona hekima ya Mungu ilikuwa ndani yake, ili afanye hukumu. Hakika ni bora mama ampe mtoto wake mtu mwingine amtunzie kuliko kumwua yule mtoto kama alivyofanya yule mwanamke wa pili! Mtoto ni zawadi toka kwa Mungu na sisi hatuna mamlaka ya kutenda kitendo chochote kile cha ukatili kwa mtoto , au mtu mzima. Daima tukiwa katika kutahayari tuombe msaada wa mashauri kwa wazazi wacha Mungu, au wale wenye hekima na watumishi wa Mungu.

Sisi si wafalme au malkia ila tunahitaji hekima katika kazi ile Mungu ametoa kwa kila mwenye mwili. Mungu hakutoa hekima kwa Sulemani tu, kwani hata leo nawe ukimwomba hekima utapewa, nami leo nimeiomba nikiandika kisa hiki. Maana ni ahadi ya Mungu kwamba kama kuna mtu amepungukiwa na hekima aombe na Mungu awapaye wote kwa ukarimu, wala hakemei, naye atapewa. Ila tuombe kwa imani, pasipo shaka yoyote ili tusiwe kama wimbi linalopelekeshwa huku na huko. Yakobo 1:5-8. Mimi nimepungukiwa hekima, niombee, nami nakuombea! Tumwombe Mungu hekima na moyo wa ufahamu. "Basi Bwana tupe sisi watumishi Wako moyo wa adili tuweze kuwaamua watu Wako, na tupate kupambanua mema na mabaya. Kwa maana ni nani awezaye kuwaamua watu Wako hawa walio wengi?". Kwa maneno mengine "Umeniweka kuwa mfalme juu ya watu Wako. Tafadhali nipe hekima niwatawale kwa uadilifu na uaminifu." Mungu alifurahishwa na ombi hili kwa sababu halikuwa la ubinafsi, bali ni jambo ambalo lingemfanya kuwa na ufanisi i katika utekelezaji wa utume Wake.

*Yote ambayo yanaweza kufanywa katika kuwaombea wagonjwa ni kumsihi tu MUNGU kwa dhati na bidii, na bila kuchoka kwa niaba yao, na kwa ujasiri kamili

kabidhi suala hilo mikononi Mwake. Ikiwa tunazingatia uovu mioyoni mwetu Bwana hatatusikia. Yeye Anaweza kufanya apendavyo na watu Wake Mwenyewe.


---

Mungu akikwambia uombe mambo matatu akupatie utachagua nini? Sulemani alipata ndoto gani? Je, Uchaguzi wa Sulemani ulimpendeza Mungu? Sulemani alionyeshaje hekima yake?

**SIKU YA 106**
**(Aprili 15)**

# Maneno ya Hekima

**- Mithali**



Siku kwa siku Sulemani alikuwa na maneno ya hekima, akazungumza mithali 3000 na nyimbo 1005. Alikuwa na mwandishi maalumu wa kumwandikia maneno haya ya hekima. Wengi hata wasio waumini wanazinukuu mithali za Sulemani leo. Kwa hekima Mungu aliyompa Sulemani, aliandika vitabu vitatu vya mashairi, na baadhi ya Zaburi. Aliandika wimbo wa Sulemani akiwa kijana, kisha Mithali na mwishowe Mhubiri akiwa mzee. Anaanza Mithali kwa kukazia kuwa "Kumcha BWANA ni chanzo cha maarifa, bali wapumbavu hudharau hekima na adabu." Hekima inakazia kuwa wenye dhambi wakikushawishi kutenda uovu, ukimbie, au kuzuia miguu yako ili usiende maovuni, usiwe mtu wa kufuata-fuata watu au kuigiza, bali uwe na msimamo. Bila shaka mithali hizi kila mtoto anapaswa akariri. Kuna tofauti kati ya maarifa au elimu na hekima. Hekima ni kupata maarifa au elimu na kuitumia vizuri kwa utukufu wa MUNGU na kusaidia watu. Soma sura moja kila siku, na kila mwezi utamaliza kitabu hiki!

"Mwanangu usisahau sheria yangu; Bali moyo wako uzishike amri Zangu. Zitakuongezea wingi wa siku. Na miaka ya uzima na amani…Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe. Katika njia zako zote mkiri Yeye. Naye atayanyosha mapito yako. Usiwe mwenye hekima machoni pako. Mche Bwana ukajiepushe na uovu. Itakuwa afya mwilini pako…Mheshimu Bwana kwa mali yako…ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi. Usidharau kuadhibiwa na BWANA… Kwa kuwa BWANA ampendaye humrudi, kama vile baba mwanawe ampendezaye." Mithali 3:1-11.

Nitaandika mithali zingine chache hapa utafakari na kujadili na wazazi wako. "BWANA atakuwa tumaini lako, Naye atakulinda mguu wako usinaswe. Usiwanyime watu mema yaliyo haki yao, ikiwa katika uwezo wa mkono wako kuyatenda. Usimwambie jirani yako, nenda, urudi halafu, na kesho nitakupa; Nawe unacho kitu kile karibu nawe. Usiwaze mabaya juu ya jirani yako, ambaye anakaa karibu nawe na kujiona salama. Usishindane na mtu bila sababu, ikiwa hakukudhuru kwa lolote." Mithali 3:26-30. Mashauri mazuri ajabu kama tukitaka

kuwa na mahusiano ambayo Mungu anataka tuwe nayo kwa wenzetu!

“Njia ya mwenye haki ni kama nuru ing’aayo, ikazidi kung’aa hata mchana mkamilifu.” Mith 4:18
Mithali 4:13 yasema “Mkamate sana elimu, usimwache aende zake; Mshike, maana yeye ni uzima wako”. Elimu ni muhimu, na maarifa haya si lazima mtu ayapate kwa kwenda darasani, maana mtu aweza kwenda shule ila asielimike. Nafikiri kinachomaanishwa hapa, ni kujifunza, kuchunguza na kujipatia maarifa ambayo yatakuwa na manufaa kwaajili ya binadamu wengine katika kukabiliana na mazingira yao. Sayansi, sanaa, teknolojia au ujuzi wowote unaotajwa hapa ni ule ambao unaendana na Muumba wetu. Maelfu ya waliovumbua vitu katika ulimwengu wetu walikuwa wacha Mungu, na hata ilinishangaza kwamba wengi walikuwa watoto wa wachungaji! Mfano Orville na Wilbur Wright waliovumbua ndege kutoka Ohio, Marekani, walikuwa waumini, na baba yao alikuwa mchungaji, hawa walikwenda pwani ya Carolina kufanyia mazoezi ndege yao, nao wakaweza kuwa hewani kwa dakika 8! Wakajua wameshinda! Eccles alivumbua jinsi seli za ubongo zinavyopeleka habari, Pascal alivumbua Kalkuleta, Lister alihusika na upasuaji uliozingatia kwa makini uwepo wa bakteria naye alipunguza vifo vingi, Leeuwenhoek alivumbua viumbe vidogo kama bakteria, Wengine ni kama Keppler wa ujerumani aliyevumbua kwamba dunia yetu ndiyo inayolizunguka jua. Galileo pia naye akavumbua Telescope ya kuona anga mbali. Boyle wa Uingereza alivumbua gesi ya asili, na mada za kemia, Faraday alivumbua mambo ya umeme. Mendel mtawa wa Chekoslovakia alivumbua siri za urithi kwenye seli zetu. Newton alivumbua nguvu za uvutano. Dalton alivumbua atomi ambayo ndiyo inatengeneza mada zote. Carver alivumbua mambo yahusuyo kilimo na hata kutengeneza siagi ya karanga. Nightingale alisaidia kupunguza maambukizo kwenye mahospitali na kusaidia kuanzisha taaluma ya uuguzi. Volta alitengeneza betri ya kwanza, Babbage alivumbua kompyuta za kwanza kwanza. Steno alikuwa mwanzilishi wa fani ya jiolojia. Morse alivumbua simu ya kwanza na hata alituma ujumbe wake wa kwanza kwa kutumia fungu la Hesabu 23:23 linalosema “Ni mambo ya ajabu iliyoje aliyoyatenda Mungu!” Beumann alivumbua hesabu za maumbo zilizomsaidia Einsten kukorokotoa hesabu yake inayojulikana sana kama E = mc2.

“Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; maana ndiko zitokako chemchemi za uzima.” Mithali 4:23.

Sulemani, akiwaangalia chungu alipata fundisho la wote wapendao uvivu. “Ewe mvivu, mwendee chungu, zitafakari njia zake ukapate hekima. Kwa maana yeye hana akida au msimamizi, wala mkuu, lakini hujiwekea akiba ya chakula wakati wa jua. Hukusanya chakula chake wakati wa mavuno. Ewe mvivu, utalala hata lini? Utaondoka lini katika usingizi wako? Bado kulala kidogo, kusinzia kidogo. Bado kukunja mikono upate usingizi. Hivyo umaskini wako huja kama mnyanganyi.” Mithali 6:6-11.
“Mtu aziniye na mwanamke hana akili kabisa; Afanya jambo litakalomwangamiza nafsi yake.” Mithali 6:32.

“Kumcha BWANA ni kuchukia uovu; Kiburi na majivuno, na njia mbovu, na kinywa

cha ukaidi pia nakichukia." Mithali 8:13.
"Nawapenda wale wanipendao, Na wale wanitafutao kwa bidii wataniona." Mithali 8:17. "Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye; Bali mwana mpumbavu ni mzigo wa mamaye." Mithali 10:1.

"Akusanyaye wakati wa mavuno ni mwana mwenye hekima; Bali asinziaye wakati wa mavuno ni mwana mwenye kuaibisha." Mithali 10:5.

"Akubaliye kurudiwa huwa katika njia ya uzima; bali yeye aachaye maonyo hukosa." Mith 10:17

"Kijapo kiburi ndipo ijapo aibu; bali hekima hukaa na wanyenyekevu." Mithali 11:2.

"Mpeleka habari za umbeya hufunua siri, Bali mwenye roho ya uaminifu husitiri mambo." Mithali 11:13.

"Mwanamke mwema ni taji ya mumewe; Bali aaibishaye ni kama kuoza mifupani mwake." Mithali 12:4.

"Mwenye haki huufikiri uhai wa mnyama wake; bali huruma za mtu mwovu ni ukatili." Mith 12:10

"Mwana mwenye hekima husikiliza mausia ya babaye; bali mwenye dharau hasikilizi maonyo." Mithali 13:11.

"Enenda na wenye hekima nawe utakuwa na hekima; bali rafiki wa wapumbavu ataumia." Mithali 13:20.

"Yeye asiyetumia fimbo kwa upendo humchukia mwanawe; Bali yeye ampendaye humrudi mapema." Mithali 13:24.

"Kila mwanamke aliye na hekima hujenga nyumba yake; bali aliye mpumbavu huibomoa kwa mikono yake mwenyewe." Mithali 14:1.

"Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu; lakini mwisho wake ni njia za mauti." Mith14: 12.

"Mjinga huamini kila neno; Bali mwenye busara huangalia sana aendavyo." Mithali 14:15. "Amdharauye mwenzake afanya dhambi; Bali amhurumiaye maskini ana heri." Mithali 14:21.

"Amwoneaye maskini humsuta Muumba wake; Bali yeye awahurumiaye wahitaji humheshimu." Mithali 14:31.

"Jawabu la upole hugeuza hasira; bali neno liumizalo huchochea ghadhabu." Mithali 15:1. "Macho ya BWANA yako kila mahali; yakimchunguza mbaya na mwema." Mithali 15:3.

“Kuwa na mali chache pamoja na kumcha BWANA; ni bora kuliko mali nyingi pamoja na taabu.” Mithali 15:16.

“Mtu wa hasira huchochea ugomvi; Bali asiye mwepesi wa hasira hutuliza mashindano.” Mith 15:18.

“Si afadhali kupata hekima kuliko dhahabu? Naam, yafaa kuchagua ufahamu kuliko fedha.” Mithali 16:16.

“Kiburi hutangulia uangamivu, na roho yenye kutabakari hutangulia maanguko.” Mithali 16:18.
“Maneno yapendezayo ni kama sega la asali; Ni tamu nafsini, na afya mifupani.” Mithali 16:24.
“Asiye mwepesi wa hasira ni mwema kuliko shujaa; na mtu aitawalaye roho yake kuliko mtu atekaye mji.” Mithali 16:32.

“Apendaye ugomvi hupenda dhambi; auinuaye sana mlango wake hutafuta uharibifu.” Mith 17:19.

“Moyo uliochangamka ni dawa nzuri; Bali roho iliyopondeka huikausha mifupa.” Mithali 17:22. “Jina la BWANA ni ngome imara; mwenye haki huikimbilia akawa salama.” Mithali 18:10. “Shahidi wa uongo hakosi ataadhibiwa; wala asemaye uongo hataokoka.” Mith19:5.
“Amhurumiaye maskini, humkopesha BWANA; Naye atamlipa kwa tendo lake jema.” Mithali 19:17.

“Hata mtoto hujijulisha kwa matendo yake; kwamba kazi yake ni safi, kwamba ni adili.” Mith 20:11.

“Usiseme mimi nitalipa mabaya; Mngojee BWANA naye atakuokoa.” Mithali 20:22.

“Ni afadhali kukaa katika nchi ya nyika; kuliko na mwanamke mgomvi, mchokozi.” Mith 21:19.

“Yeye ajibuye kabla hajasikia ni upumbavu na aibu kwake.” Mithali 18:13.

“Heri kuchagua jina jema kuliko mali nyingi; Na neema kuliko fedha na dhahabu.” Mithali 22:1.

*Mara nyingi imekuwa upendeleo wangu kuomba na wagonjwa. Tunapaswa kufanya hivi mara nyingi zaidi kuliko tunavyo fanya.

Mtoto anajulikanaje tabia zake mbele ya watu? Kwa nini mtu mgomvi na mchokozi watu humwepuka? Kulipiza kisasi ni kazi ya nani? Kwa nini hasira ni mbaya? Kwanini tusome Mithali? Kuna tofauti gani kati ya ujuzi, elimu na hekima?

**SIKU YA 107**
**(Aprili 16)**

# Mithali na Mhubiri




Sulemani aliendelea kuandika, mambo ya kutusaidia sote, watoto kwa wakubwa. "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee." Mithali 22:6. "Ujinga umefungwa ndani ya moyo wa mtoto; lakini fimbo ya adhabu itaufukuzia mbali." Mith 22:15.

"Je! Wamwona mtu mwenye bidii katika kazi zake? Huyo atasimama mbele ya wafalme." Mith 22:29.

"Msikilize baba yako aliyekuzaa, wala usimdharau mama yako akiwa mzee. Inunue kweli wala usiuze, Naam, hekima mafundisho na ufahamu? Mith 23:22, 23.

"Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima" Mith 20:1. Soma na Mithali 23:29-35. Kamwe usionje kileo.

"Mguu wako usiingie katika nyumba ya jirani yako ila kwa kiasi; Asije akakulaani na kukuchukia." Mith 25:17.
"Adui yako akiwa na njaa mpe chakula; Tena akiwa na kiu, mpe maji ya kunywa. Maana utamtia makaa ya moto kichwani pake; na BWANA atakupa thawabu." Mithali 25:21, 22.

"Mtu mvivu husema, simba yuko njiani; simba yuko katika njia kuu." Mithali 26:13.

"Mtu apitaye na kujisumbua kwa ugomvi usio wake; Ni kama mtu ashikaye mbwa kwa masikio yake." Mithali 26:17.

“Usijisifu kwa ajili ya kesho; maana hujui yatakayozaliwa na siku moja.” Mithali 27:1

“Jeraha utiwazo na rafiki ni amini; bali kubusu kwa adui ni kwingi sana.” Mithali 27:6.

“Waovu hukimbia wasipofuatiwa na mtu; Bali wenye haki ni wajasiri kama simba.” Mith 28:1.

“Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; Bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema.” Mithali 28:13.

“Aibaye mali ya babaye au mamaye, na kusema si kosa; Mwana huyo ni rafiki wa mtu mharibifu.” Mithali 28:24.

“Aonywaye mara nyingi akishupaza shingo, atavunjika ghafla, wala hapati dawa.” Mithali 29:1. “Je, umemwona mtu mwenye kuhamaki katika maneno? Afadhali kumtumaini mpumbavu kuliko yeye. Mith 29:20.

“Uniondolee ubatili na uongo; usinipe umaskini wala utajiri; unilishe chakula kilicho kadiri yangu. Nisije nikashiba nikakukana, nikasema BWANA ni nani? Wala nisiwe maskini sana nikaiba, na kulitaja bure jina la Mungu wangu.” Mithali 30:8, 9.

Tukiyajua na kuishi mausia ya Mithali kama alivyoagiza tutakuwa na mafaniko, furaha na baraka. Maandishi haya ya Mithali, si hekima za Sulemani, bali ni hekima ya Mungu Mwenyewe aliyomvuvia Sulemani kuandika!

Sulemani alikuwa ana hekima na akili kupita wote, pia alikuwa na mali. Talanta hizi alizitumia kufanya utafiti ili ajue kwamba mtu ana faida gani kwa kazi yake aifanyayo chini ya jua. Akatoa hitimisho kwamba ni ubatili mtupu, ubatili mtupu, mambo yote ni ubatili. Hii haimaanishi kwamba Mungu hakutuumba tupate furaha, bali Sulemani anatueleza kwa undani ili tusifanye makosa kama yeye aliyoyafanya. Kwa sababu ametupatia majibu ya kweli kwenye uchunguzi aliofanya ili sisi tusianguke kama yeye. Anasema mambo yote ni yale yale, yamejaa uchovu, hakuna jipya, yanajirudia tu, asubuhi, mchana, jioni, asubuhi, mchana, jioni. Ni kukimbiza upepo, au kupiga ngumi upepo; ni kubeba maji kwenye nyavu. Ni kama mtu anayeendesha baiskeli ya kunoa vyuma, haendi kokote. Wengi wasiomjali Mungu wanafikiri kitabu hiki kinaunga mkono mtindo wao wa maisha! La! Hasha. Kila andiko la Mungu limevuviwa kuwa msaada wa mafundisho kwetu, ili kutuweka kwenye misingi ya kuishi juu ya jua milele, na si chini ya jua tu!

Anasema mtu akiwa na mali, hata afanye kazi ni shida tu maana anafanya watu wamwonee wivu, hata hivyo, yote ni mabua maana moyo na hata roho yake inaendelea kuwa na matundu ya huzuni. Anaweza kucheka ila anaficha huzuni ndani ya moyo. Japo yeye alikuwa na watumwa, mali, ngombe, vinywaji, vyakula vitamu vitamu, wachekeshaji, bustani, chemchemi, elimu, kwaya, bendi, na mengine, hivi vitu vilimkinaisha. Watu wa kisasa wanaishi na kelele nyingi, na shughuli nyingi ili kujisahaulisha upweke chini ya jua. Augustine alisema, “Wewe Mungu umetuumba kwa ajili yako, hivyo mioyo yetu inatangatanga mpaka tupate pumziko litokalo kwako.” Kuna wimbo usemao imani yangu imepata pumziko kwako. Njaa kwenye

roho zetu zitashibishwa tu na kumjua Mungu na kumtumikia, na si tamaa au anasa za utotoni au ujanani. Tumia nguvu zako na hali yako kuhudumia wenye mahitaji, kumtumikia Mungu kwa kuwa mmisionari mahali unapoishi, na kuhudhuria. Usipoteze muda wako kufanya mambo ya kipuuzi, bali fanya uwekezaji juu ya jua. Soma Mathayo 5 uone furaha halisi chini ya jua, utaona kuwa wana heri wale walio maskini wa roho, wana heri wale walio wapatanishi, wana heri wale walio na njaa na kiu ya haki, wana heri wale wenye moyo safi. Furaha haitokani na kufanya mapenzi yetu na kujitukuza wenyewe. Kununua vitu na kuvitupa, na kwenda kununua vingine, ni njia moja ya kujisahaulisha huzuni zetu. Vitu havitupatii furaha, bali uhusiano na BABA yetu wa mbinguni.

Kuna siku ambayo matendo yetu yote chini ya jua, ya wazi na ya siri, yataonekana kwenye kitabu cha kumbukumbu. Toa huduma kwa upendo, furaha na baraka tele zitakurudia.

*Ni jukumu letu kuwasilisha wagonjwa na wanaoteseka kwa Kristo mikononi mwa imani yetu .... Tunapaswa kushikilia ahadi Yake, na kuomba kwa ajili ya udhihirisho wa nguvu Zake. Kiini cha injili ni urejesho/kurejeshwa, na Mwokozi angetutaka tuwaombee wagonjwa, wasio na tumaini, na wenye shida washizishikilie nguvu Zake.

---

Afichaye dhambi zake nini kitamtokea? Mithali 7 inasema mwanamke mwovu ana tabia gani? Mithali 31 inasema mwanamke mwema ana tabia gani? Je, msichana mwovu au mvulana mwovu ana tabia gani? Kwa nini bidii ya kazi ni muhimu? Mtu awezaje kumkopesha BWANA? Ubatili na chini ya jua ina maana gani? Kuna tofauti gani kati ya vita na kugombana? Adui zetu tuwatendeeje?

**SIKU YA 108**
**(Aprili 17)**

# Mhubiri au Kohelethi

Kitabu cha Mhubiri kina mafundisho kwa watoto na watu wazima kwa pamoja. Mwandishi anasema, Wewe kijana ufurahie ujana wako, moyo wako ukuchangamshe, lakini yote yataletwa hukumuni… ujana au utoto ni ubatili na pia utu uzima. Ameona maisha ni kitendawili, na huwa hayana kuridhika, ni mzunguko unaoonekana hauna malengo, kwani watu huzaliwa na kufa, huzaliwa na kufa. Alitaka jibu la 'maana ya maisha' ambalo ndiyo swali letu leo.

Akiwa ameishi miaka mingi, Sulemani, aligundua kwamba kila kitu kina wakati wake. Wakati wa kutupa na wakati wa kuokota, wakati wa kulia na kucheka, kutafuta na kupoteza, kung'oa na kupanda, kubomoa na kujenga, kurarua na kushona, kunyamaza na kunena, vita na amani au kupenda na kuchukia. Akagundua kuwa "hakuna jipya chini ya jua" ambalo binadamu atajivunia kwamba yeye ndiye wa kwanza kuliona.

Akaona kwamba katika wingi wa hekima mna wingi wa huzuni, na ukiongeza maarifa unaongeza masikitiko, kama si kwa ajili ya kumcha BWANA. Yeye alitaka kuburudisha moyo wake kwa kujenga nyumba, kupanda miti ya matunda, kufuga nyani kama maburudisho ya moyo, kununua wajakazi, kuwa na mali na mifugo mingi, waimbaji wa kumwimbia, wanawake wa kumfurahisha, dhahabu na mengineyo, wala hakuzuia moyo wake katika furaha yoyote , lakini kwa kukosa kiasi, akagundua kuwa yote ni ubatili au kama vile kula upepo tu, haileti furaha au faida. Mwishowe akachukia yote hayo aliyohangaikia kwani baada ya kazi yake na yote aliyokuwa nayo, hakuna kumbukumbu la milele la mwenye hekima, na jinsi anavyokufa mwenye hekima na mpumbavu ni sawa tu. Yaani baada ya kushughulikia yote atakufa na kumwachia anayefuata, naye akiwa mpumbavu ataharibu yale yote aliyojishugulisha nayo kwa hekima na uangalifu, basi akaona ni ubatili. Mwishowe aliona ale na afurahie maisha bila kujisumbua na kujichoma kwa maumivu mengi ya tamaa. Alitoa hitimisho la utatuzi akisema, "Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako, kabla hazijaja siku zilizo mbaya… utakaposema mimi sina furaha katika hiyo." Jumla ya maneno yote ya muhimu aliona ni kumcha Mungu na kuzishika amri Zake; maana kwa jumla, ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya.

Nanyi watoto na vijana, kila kitu kinapita ila kumcha Mungu na kuzishika amri zake ndicho kitu pekee muhimu na cha kudumu. Katika Kohelethi au Mhubiri, anatafakari maisha ni nini? Ni kitabu cha maisha ya mtu. Anaelezea vile vya muhimu, akiangalia malengo ya maisha yake na matokeo yake. Kwa wale watu wazima wanaelewa kabisa anachozungumza kwani kila mtu anakaa na kuwaza alivyojisumbua na mengi, na anapotathmini anaona yote ni ya kupita tu. Safari yake ni ya binadamu wote. Akiwa mzee na amesafiri na kupita kwingi, anakubali

au kugundua muhtasari wa furaha, ni kuridhika, na maana ya maisha ni moja tu "Mche Mungu nawe uzishike amri Zake, Maana kwa jumla ndiyo impasavyo mtu." Alijaribu kufanya mambo mengi ili apate furaha, lakini aliona ni ubatili au kujilisha upepo. Huzuni au sonona ikamvamia, maisha yalikuwa tupu, yasiyokuwa na faida (ubatili). Vyote havikumridhisha moyo wala kumpatia furaha. Furaha ya dunia na vitu vyake ni vya muda mfupi tu. Ametumia neno "chini ya jua" mara 27 akimaanisha duniani. Alikunywa au kujiburudisha kushinda wote, ila bado alijisikia mtupu. Ametumia neno ubatili au kufukuza upepo mara 38, akitilia mkazo kwamba kama hakuna wokovu toka kwa Mungu, au hakuna Mungu basi hakuna maana au sababu ya maisha chini ya jua.

Watu wengine wanamtufuta Mungu usiku na mchana wakiona mambo yameharibika, au wana shida fulani ya ufukara au mali. Mara zingine kwenye nchi zilizoendelea, mtu anapojiweza anaishi maisha ya kumkufuru Mungu. Hata nasi japokuwa hatujiwezi, siku tukijiweza, ule ubinafsi unaibuka na pembe zake zinaonekana kwa wengine kwa kutaka kujitukuza na kuwa na vitu. Hata wale jirani zetu wenye mahitaji hatuwajali. Tunaweza kuwapa vitu vichakavu tulivyovichoka, hatimaye tunagundua kuwa vitu havitupatii furaha ya kweli.

Je, maisha yako hayana maana au malengo? Nakushauri umweke Mungu mbele katika kila kitu, awe wa kwanza, aliye bora na aliye kila kitu kwako. Lenga mbingu na siyo anasa za muda zinazopita haraka. Mtafute kwanza Mungu na haki yake, na vyote utazidishiwa, hiyo ni pamoja na furaha. Kuna huzuni kutafuta vitu vya dunia tu bila kumpenda na kumtafuta Mungu wa mbinguni. Kumwamini Mungu ndiyo njia pekee ya kupata maana ya maisha, vingine vinachakaa haraka.

Kila anapotafuta kitu na akikipata anakiweka kabatini, na kuanza kufukuzia kingine, maana alicho nacho hakuridhika nacho. Vitu vinakuwa vimejaa 'kabatini au ghalani.' Pengine ni wanasesere, nguo, nyumba, magari, boti, vyombo na vitu vingine, lakini havimpi furaha, na anaendelea tena kutafuta akifikiri atapata raha, mwishowe anakinai kila kitu. Huenda nasi pia tunasema, nikimaliza shule ndiyo nitakuwa na furaha. Nikipata kazi ndiyo nitakuwa na furaha. Nikioa au kuolewa ndiyo nitakuwa na furaha. Nikipata watoto ndiyo nitakuwa na furaha. Watoto wakitoka kwangu na kujitegemea ndiyo nitakuwa na furaha. Nikistaafu ndiyo nitakuwa na furaha. Nikipata wajukuu ndiyo nitakuwa na furaha. Daima furaha tunaikimbiza, ila hatuishiki. Hata hivyo kesho haikuahidiwa kwetu, ni nani ajuaye kwamba tutalala usingizi wa mauti na tusipate vile tunavyokimbizana navyo? Basi vitu visitujae mioyoni kiasi kwamba tunasahau tuko hapa duniani kwa kusudi gani, tunaenda wapi, na tufanye matayarisho gani ili siku moja tuingie mbinguni.

Mwishowe Sulemani aliona kwamba katika wingi wa hekima mna wingi wa huzuni, na ukiongeza maarifa unaongeza masikitiko, kama si kwa ajili ya kumcha BWANA. Maana alitaka kuburudisha moyo wake, alikuwa na pesa zote za kukidhi anasa au haja za moyo wake. Alikuwa na mamlaka makubwa, hivyo hakuna aliyeweza kumkataza asifanye alichotaka. Akitaka farasi 1000 alipata, akitaka kupiga watu aliweza. Akitaka kulala siku nzima asifanye kazi alifanya vile. Akitaka kula kwa ulafi nyama sufuria nzima alikuwa na uwezo huo. Maisha yasiyo na wigo

ni ya hatari sana, na ndiyo maana inakuwa rahisi kwa matajiri na watawala wengi kuingia katika dhambi nzito kirahisi sana. Wanahistoria wengine walisema Sulemani alikuta ufalme ukila milo miwili kwa siku, naye akaongezea wa tatu, na milo mitatu kwa siku bila kazi ni laana kwa mwili, maana inafanya tuwe walafi, wenye afya mbaya na tusiotawala tamaa za mwili za aina yote!

Sulemani anatoa hitimisho kuwa, "Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako, kabla hazijaja siku zilizo mbaya… utakaposema mimi sina furaha katika hiyo." Jumla ya maneno yote ya muhimu aliona kuwa ni "Mche Mungu nawe uzishike amri Zake; maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likuwa jema au likiwa baya."

Kila kitu kinapita ila kumcha Mungu na kuzishika amri Zake ndicho kitu pekee kitakachodumu milele. Tusome kisa cha mfalme huyu na maanguko yake na alichojifunza ili tusirudie taabu yake. Hakuna asiyehitaji hekima, wadogo kwa wakubwa, wote tunahitaji hekima wakati wote, hakuna aliyefika maana mazingira tofauti yanatubidisha tuamue mambo katika njia tofauti, hakuna anayeipitia njia ile ile kila wakati.

*Maombi kwa ajili ya Wagonjwa yanafaa Leo kama katika Nyakati za Biblia—Mponyaji wa Mbinguni Yuko katika chumba cha wagonjwa; Anasikia kila neno la maombi yanayotolewa Kwake katika usahili wa imani ya kweli. Wanafunzi Wake leo wanapaswa kuwaombea wagonjwa, kama walivyofanya wanafunzi wa kale. Na kutakuwa na uponyaji; kwani "ombi la imani litawaokoa wagonjwa."

---

Nini maana ya Kohelethi? Sulemani alindika vitabu gani? Kwa nini vitu haviwapi watu furaha kama wanavyofikiri? Nini kinamletea mtu furaha ya kweli na ya kudumu? Kwa nini tumkumbuke Muumba wetu wakati tu vijana? Kwa nini watu wengine hufika uzee wakiwa hawajiwezi na ndiyo wanaona muda huu wa 'makapi' ndiyo warudi kwa Mungu? Kwa nini kutokuwa na kiasi ni dhambi? Je, furaha isiyo na kikomo inapatikana tukimaliza shule, tukioa au kuolewa, tukipata watoto, au tukistaafu?

**SIKU YA 109**
**(Aprili 18)**

# Kujenga Hekalu

**- 1 Wafalme 5 na 2 Mambo ya Nyakati 1, 3**

Chini ya ufalme wa Sulemani, Israeli ilipata amani na utajiri kuliko wakati mwingine wote. Sulemani akakusanya magari na wapanda farasi, naye alikuwa na magari 1400 na wapanda farasi 12,000. Akafanya fedha na dhahabu kuwa kama mawe humo Yerusalemu na mierezi akaifanya kuwa kama mikuyu. Nao farasi wa biashara wakaletwa kwake toka Misri, akawachuuza.

Hiramu, mfalme wa Tiro, alimpenda Daudi na aliposikia kuwa amefariki na Sulemani mwanawe anatawala, alituma ujumbe wa kibalozi wa kumtakia heri Sulemani. "Kwa sababu BWANA awapenda watu Wake, amekufanya uwe mfalme juu yao." Naye akamwambia kuwa wakati wa baba yake kulikuwa na vita, ila sasa yeye ana amani na anakusudia kujenga nyumba ya BWANA. Basi Sulemani akakusudia kujenga nyumba kwa Jina la BWANA na kuujengea ufalme wake nyumba. Na kwa ile amani ya kutokwenda vitani, Sulemani akapata watu 70,000 wachukue mizigo, na watu 80,000 wawe wachonga mawe, na watu 3600 wawe wasimamizi wao. Sulemani akatuma watu kwa Hiramu, mfalme wa Tiro, amsaidie mierezi kama alivyompa baba yake ili ajenge nyumba Yake. Akamwambia Hiramu kwamba anajenga nyumba ya BWANA, Mungu wake. Akamwambia Nyumba atakayoijenga ni kubwa, kwa sababu Mungu ni mkuu kuliko miungu yote. Nami ni nani basi hata nimjengee nyumba isipokuwa kwa ajili ya kufukiza fukizo mbele zake. Akaomba mafundi stadi wa kazi mbalimbali, mfano, wa michoro, dhahabu, fedha, shaba, chuma, rangi, nk. Uhusiano wa namna hii wakati mwingi una mazuri yake, kwani ushirikiano katika kazi na habari njema vinasonga mbele!

Akasema watumishi wa Hiramu wamkatie mierezi ya Lebanoni kisha walete kwa maji mpaka Yafa, naye atawapa ujira jinsi Hiramu atakavyosema, maana hakuna ajuaye kukata miti kama Wasidoni. Hiramu alifurahi na kusema ahimidiwe BWANA aliyempa Daudi mwana mwenye akili juu ya watu wengi, akamwambia atafanya kama Sulemani alivyoomba kwa miti ya mierezi, miberoshi na mambo mengine. Watumishi wake wataishusha mpaka baharini na kuiendesha mpaka pale watakapoagizwa, na huko wataifungua ili yeye aichukue. Akamwambia awape chakula watu hawa, naye Sulemani akatuma chakula kama vile ngano, shayiri, mafuta, na vingine, nao wakafanya maagano. Watu wakatumwa Lebanoni 30,000 wakagawanya sehemu tatu na kutumwa 10,000 Lebanoni kwa zamu ya mwezi mmoja, na miezi miwili wakakaa nyumbani. Mfalme akaamuru yaletwe mawe makubwa yaliyochongwa ya kuweka msingi, na waashi wa Hiramu na Sulemani ndiyo walioyachonga kabla ya kuyapeleka kwenye ujenzi. Wakaweka miti tayari kwa kujenga nyumba. Akatumwa Huramu, mwana ambaye mama yake alitoka kabila la Dani ila baba yake alitoka Tiro. Huyu naye alijaa roho ya hekima ya ufundi, ajuaye kazi ya shaba, kuchora, chuma, mawe, miti, urujuani, samawi, kitani,

na nyekundu, pia hufikiri na kubuni ustadi. Huyu alikuwa na ujamaa kwa mbali na Aholiabu, aliyekuwa msaidizi wa Bezazeli aliyejenga hekalu jangwani. Mojawapo ya kazi nzito za kufikiri na ustadi alizofanya Huramu ni kutengeneza mihimili miwili ya shaba mbele ya hekalu, ya futi 33 na upana futi saba. Akatumia udongo wa mfinyazi, kutoka bonde la Yordani, akazinyanyua na kuzipeleka Yerusalemu. Hizi zilisimama mamia ya miaka kwa utukufu wa Mungu zikikumbusha kuwa mtu anapojitoa kufanya kazi ya Mungu, Mungu humpatia karama na uwezo. Tunapozungumzia fahari ya hekalu la Sulemani, hatusahau talanta ya mtu huyu. Hiramu alitengeneza vitu vingine kama bakuli la futi 18 kwa 9, lenye ujazo wa lita 6000 hivi. Alitengeneza makomamanga 400 ya shaba, vitako, koleo, n.k. alikuwa na madhaifu yake, ila alitumia talanta yake kwa kazi ya Mungu.

Ninajaribu kufikiria jinsi watu hawa wengi walioshugulikia ujenzi wa hekalu, kwamba walilala wapi? Je! walikuwa na maji ya kutosha kwa kunywa na usafi? Nani aliwapikia wote? Je! Walikuwa na 'hospitali' kwa waliojeruhiwa? Je! Familia nzima zilikwenda au wake na watoto walibaki? Orodha ya maswali inaendelea……. Ninashangaa hata jinsi 'vyoo' na 'bafu' zilivyojengwa! Hakika Mungu ni wa kushangaza jinsi anavyofanya kazi zote kwa utaratibu. Nasi pia tunaweza kujenga hekalu kwaajili ya Bwana, miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu. Je, unajua jinsi ya kutunza mwili wako kutokana na maagizo ya Biblia? Je, unakula chakula unachopaswa, Je, unafanya mazoezi? Je, unapata hewa bora, Je, unamtegemea Mungu? Je, unakunywa maji glasi sita mpaka 10 kwa siku? Je? unafanya mambo kwa kiasi? Je, Unasoma Maandiko na kuomba kila siku?

Mawe yote yalikatwa kabla ya kupelekwa kwenye ujenzi. Ujenzi ulikuwa kimya kimya, "wala nyundo, wala shoka, wala chombo chochote cha chuma sauti yake haikusikiwa ilipokuwa ikijengwa nyumba" ya BWANA. Pengine Bwana alitaka kuonyesha mfano wa kazi ya Kanisa Lake likifanya kazi bila, makelele kwa kuongozwa na Roho wake. Watoto wakumbuke hili, wakiwa kwenye ibada kanisani, wasifanye kelele. Soma zaidi kwenye Shuhuda Gombo la Tano, Sura ya 55, Mwenendo ndani ya Nyumba ya Mungu. Leo Mungu anajenga hekalu jingine, yaani miili yetu, miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu ambamo Bwana hukaa, basi tulapo tunywapo au tutendapo Neno lolote, tufanye kwa utukufu wa Mungu.

Sulemani akaanza kuijenga nyumba ya BWANA kwenye mlima Moria. Hekalu likajaa mlima wote, mwaka wa 480 tangu Waisraeli watoke nchi ya Misri, katika mwaka wa nne wa kutawala kwake. Mwaka wa nne msingi uliwekwa na ujenzi ukamalizika baada ya miaka saba, ila mambo yote kwisha kabisa hata madogo kumalizika kabisa ilichukua miaka kumi na moja. Baba yake Sulemani, alikuwa amechora hata mchoro wa hekalu na kufanya mipango mingi kama kuandaa talanta 3000 za dhahabu na 7000 za shaba. Siku zake za mwisho alipokuwa akiwaaga watu, wengine wakatoa nao sadaka zao za hiari kwa ajili ya kujenga hekalu.

Uhusiano kati ya Daudi na Hiramu, na Sulemani na Hiramu unatoa tamko lenye nguvu kwa ajili ya ushirikiano ambao kanisa la Masihi leo linaweza kufanya na wale wasioamini. Walakini, kuna tahadhari ambazo zinapaswa kuzingatiwa wakati wa kuunda miungano kama hii:

1. Usijifungie kwenye maelewano yasiyoendana na kanuni za Maandiko Matakatifu
2. Wakati wowote tunapofanya biashara na mtu yeyote asiye msafiri wa mbinguni, ni lazima tuichukue kama kazi yetu ya umishonari kumkaribisha aende nasi mbinguni.
3. Mara nyingi tunapata stadi nzuri kutoka kwa watu wasio waumini, nasi pia tunawafundisha kuhusu wokovu. Hili lilitokea kwa Yusufu huko Misri, na Danieli, Hanania, Mishaeli, Azaria huko Babeli.

*Mungu Yuko tayari kurejesha afya ya wagonjwa sasa kama vile Roho Mtakatifu aliposema Maneno haya kupitia mwandishi wa-Zaburi. Na Kristo Ndiye yule yule daktari/tabibu mwenye huruma sasa kama alivyokuwa wakati wa huduma Yake hapa duniani. Ndani Yake kuna zeri ya uponyaji kwa kila ugonjwa, nguvu ya uponyaji kwa kila udhaifu. Wanafunzi Wake kwa wakati huu wanapaswa kuwaombea wagonjwa kweli kama vile wanafunzi wa zamani walivyoomba. Na uponyaji utafuata; kwani "ombi la imani litawaokoa wagonjwa." Tunayo nguvu ya Roho Mtakatifu, uhakika mtulivu wa imani, ambao unaweza kudai ahadi za MUNGU. Ahadi ya Bwana, "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya" (Marko 16:18), hili ni la kuaminika sasa kama katika siku zile za mitume. Inaonyesha fursa ya watoto wa MUNGU, na imani yetu inapaswa kushikilia yote ambayo tungeweza kuyashikilia. Watumishi wa Kristo ndio mfereji wa utendaji Wake, na kupitia kwao anatamani kutumia nguvu Zake za uponyaji. Ni jukumu letu kuwasilisha wagonjwa na wanaoteseka Kwake Mungu, kwenye mikono ya imani yetu. Tunapaswa kuwafundisha kuamini katika Mponyaji Mkuu.

---

Hiramu alituma ubalozi na ujumbe gani? Mfalme wa Tiro alitoa nini? Mfalme Sulemani alitoa nini? Huramu fundi alikuwa na ustadi gani? Kwa nini sauti ya kugonga gonga haikusikia kwenye ujenzi wa hekalu? Orodhesha jinsi tunavyopasa kuenenda ndani ya nyumba ya Mungu. Je, unafikiri bila amani na umoja tunaweza kumaliza kazi ya injili leo?


**SIKU YA 110**
**(Aprili 19)**

# Ujenzi wa Hekalu Wakamilika

**- 1 Wafalme 6-8**

Jiwe hata jiwe likaweka na kuenea na kukaa vizuri. Watoto wakaja kulitazama, na kila mtu akastaajabu, maana lilikuwa la fahari, ambayo haijapata kuonekana. Watu waliangalia ukimya na utulivu pia. Daudi alikuwa ameanza kazi yake miaka mingi kabla, kwa kukusanya vifaa. Hekalu lilikuwa na baraza au nyua mbili, ua wa mbele lilikuwa la Waisraeli wanaume kuingilia ila hawakuruhusu wageni, na mbele ya baraza hilo kulikuwa na baraza kwa makuhani peke yao.

Vipimo vya hema ya kukutania ya Musa ilikuwa futi 55 urefu, futi 18 upana na futi 18 kwenda juu.
Vipimo vya Hekalu lililojengwa wakati wa Sulemani lilikuwa futi 110 urefu, upana futi 36 na kwenda juu futi 36.



Hekalu la Sulemani, pia liligawanywa sehemu mbili, patakatifu na patakatifu pa patakatifu. Paa lilikuwa la mierezi na sakafu ya miberoshi, hakuna jiwe lililoonekana. Mbao zilifunikwa kwa dhahabu. Milango ilikuwa ya dhahabu na mifano ya makerubi kwenye ukuta iliyonakishiwa na mitende na maua yaliyofunika. Mapazia yalikuwa ya rangi ya bluu, zambarua, na nyekundu. Makerubi wa patakatifu pa patakatifu walitengenezwa kwa mbao za mzeituni. Madhabahu ya uvumba yalikuwa ya dhahabu na hata meza ya mikate ya wonyesho na kinara cha taa vilikuwa vya dhahabu. Rangi zilikuwa za kupendeza ajabu. Nje ya hekalu kulikuwa na madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa na birika la kutawadha. Kila mtu, kuanzia mfalme mpaka mchukua mizigo walikuwa wamefanya kazi yao na kumpa Mungu utukufu. Usidharau kazi ndogo unayopata, nayo inahitajika ili kitu kizima kiwe kamili. Mwombe Mungu akusaidie kuifurahia na kuifanya kwa uaminifu.

Kilichobakia ikawa ni kuleta sanduku la agano kutoka mji wa Daudi. Na kisha kuweka hekalu wakfu. Lazima kulikuwa na maandamano makubwa na furaha watu walipoona sanduku la agano, ambalo sasa lilikuwa na miaka kama 480 likiletwa

kwa kicho na walawi. Walileta vyombo vitakatatifu vya hekalu lile na kuviweka kwenye jengo jipya. Wakaleta sanduku na kuliweka ndani, japo lilikuwa dogo na bila vitu vingi, isipokuwa mbao za Musa za Mlima Sinai, lakini lilikuwa ndicho kitu cha thamani kupita vyote kwenye hilo hekalu, maana bila sheria ya Mungu, na kiti cha rehema, huduma zote za hekalu hazingekuwa na maana yoyote.

Sulemani akaviingiza vile vitu alivyovitakasa Daudi baba yake, yaani, fedha, dhahabu na vyombo, akavitia ndani ya hazina za nyumba ya BWANA.

Sulemani akawakusanya wazee wa Israeli kwa makabila yao wamwendee huko Yerusalemu, ili wapandishe sanduku la agano la BWANA toka mji wa Daudi, yaani, Sayuni. Wakakutana kwa mfalme kwenye sikukuu, na makuhani Walawi wakaja na kujitwika sanduku. Wakalipandisha sanduku na ile hema ya kukutania na vyombo vitakakatifu vilivyokuwa ndani. Walichinja sadaka za kondoo na ng'ombe wasioweza kuhesabika wala kufahamika idadi yao kwa kuwa wengi.

Makuhani wakaleta sanduku chini ya mabawa ya makerubi, kwa maana makerubi yalinyosha mbawa zao, juu ya mahali pa sanduku na miti yake kwa juu. Ikawa makuhani walipotoka katika patakatifu, nyumba ya BWANA ikajaa wingu. Hata makuhani hawakuweza kusimama ili kufanya huduma yao, kwa sababu ya wingu lile, kwa kuwa nyumba ya BWANA ilikuwa imejaa utukufu wa BWANA. Ndipo Sulemani akanena, "BWANA alisema ya kwamba atakaa katika giza nene. Hakika nimekujengea nyumba ya kukaa iwe mahali pa makao yako milele." Jengo lilikuwa zuri ila zile huduma za kumwabudu Mungu kwa unyofu ndiyo zilikuwa za umuhimu kuliko hata lile jengo lenyewe.

*"MUNGU anajua mwisho tangu mwanzo. Anajua mioyo ya watu wote. Anasoma kila siri ya roho. Anajua kama wale ambao wanaombewa wangeweza au wasingeweza kustahimili majaribu ambayo yangewajia wanapoendelea kuishi. Anajua kama maisha yao yatakuwa mbaraka au laana kwao wenyewe na kwa ulimwengu. Hii ni sababu moja kwa nini, wakati tunawasilisha ombi letu kwa bidii, tunapaswa kusema, "Walakini sio mapenzi yangu, bali Yako yatimizwe."

---

Sanduku la agano lililetwa kutoka wapi? Sanduku la agano lilikuwa na vitu gani viwili muhimu? Kulitokea nini makuhani walipotoka katika patakatifu? Ilichukua miaka mingapi kujenga hekalu? Sulemani alitumia miaka 7 kujenga hekalu na miaka 14 kujenga nyuma yake, unafikiri kwanini nyumba yake ilichukua muda mrefu?

**SIKU YA 111**
**(Aprili 20)**

# Hekalu Lawekwa Wakfu

**- 1 Wafalme 8-9 na 2 Mambo ya Nyakati 4-6**

Kazi ilipoisha Mfalme aliwaita wazee wa Israeli na wakuu wa kabila za Israeli huko Yerusalemu ili wapandishe sanduku la agano la Bwana toka mji wa Daudi na vyombo vitakatifu vilivyokuwamo hemani. Kisha wakachinja dhabihu ya kondoo na ng'ombe wasiohesabika kwa kuwa walikuwa wengi. Makuhani wote walienda patakafitu maana walikuwa wamejitakasa, wala hawakuzishika zamu zao. Na Walawi waimbaji chini ya Asafu na Hemani na Yeduthuni walikuwa wamevaa kitani wakiwa na vinanda na vinubi wakisimama upande wa mashariki wakipiga panda, na kuimba. Walimsifu BWANA, wakapaza sauti, na panda, matoazi na vinanda wakimsifu BWANA. Waimbaji walikuwa wengi, hata Hemani, mwonaji wa mfalme na watoto wake walikuwa waimbaji hekuluni. Makuhani hawakuweza kusimama ili kufanya huduma yao, kwa sababu lile wingu lilifunika nyumba ya BWANA. Nyumba ilijaa utukufu.

Mfalme akageuza uso wake na akawabariki mkutano wote wa Israeli, na mkutano wote wakasimama. Naye akasema, BWANA Mungu wa Israeli, ahimidiwe, aliyenena na baba yake Daudi na kulitimiza agano kwa mikono yake yeye Sulemani. Akasema toka walipotoka Misri, hakuchagua mji wowote wa kabila la Israeli, kujenga madhabahu. Lakini sasa ameuchagua Yerusalemu, ili Jina lake liwe humo. Akakumbushia kwamba likuwa moyoni mwake Daudi baba yangu kujenga hekalu, ila BWANA alisema umefanya vyema kuwaza hivi moyoni mwako. Lakini si wewe utakayejenga ila mwanao Sulemani, na BWANA amelitimiza agano lake. Naye Sulemani akasema, "nami nimesimama mahali pa Daudi baba yangu, nikiketi kwenye kiti cha enzi na kujenga nyumba ya BWANA, Mungu wa Israeli. Ndimo nilimoweka hilo sanduku, ambalo ndani yake mna agano la BWANA alilolifanya na wana wa Israeli." Akasimama mbele ya mkusanyiko wa watu wote wa Israeli na kunyosha mikono yake kwenye mimbari ya shaba akaikunjua mikono yake kuelekea mbinguni akaanza kusali akisema, "Ee BWANA, Mungu wa Israeli, hakuna Mungu kama wewe mbinguni wala duniani, ushikaye maagano na rehema kwa watumishi wako, waendao mbele zako kwa moyo wao wote." Akarudia ahadi ambayo Mungu alitoa kwa baba yake ya kwamba hatakosa kuwa na mtu wa kumrithi katika kiti cha utawala cha Israeli, na kwamba Mungu amelithibitisha agano hili na hata sasa amejenga hekalu. Lakini akakumbusha, akisema "Lakini Mungu Je! Yamkini atakaa na watu duniani? Tazama, mbingu hazikutoshi; siuze nyumba hii niliyojenga. Walakini umwangalie mtumwa wako anayoyaomba nakusihi, Ee BWANA, Mungu wangu usikie kilio na maombi anayoomba mtumwa wako mbele yako. Akaendelea kuomba ombi linalosemekana kuwa ndiyo ombi refu kupita yote katika Biblia. Kwa kifupi aliomba:

1) Hekalu liwe mahali pa msamaha na kusamehewa.

2) Watu wakija kutoa kiapo basi wasaidiwe hukumu na kulipiza mwovu ili kutenda haki.

3) Kusaidiwa wakishindwa na kupigwa na maadui zao wakija hekaluni na kuomba msamaha na kukiri, basi wasikiwe na kusamehewa dhambi yao.

4) Wakiwa na ukame, wakiomba msamaha na kuacha dhambi wasikiwe.

5) Wakiwa na majanga kama tauni, njaa ukungu, nzige au panzi, wakinyosha mikono hekaluni BWANA asikie.

6) Mgeni au mtu asiye Mwisraeli akija kuomba asikiwe.

7) Kuomba ushindi wakienda vitani au wachukuliwapo mateka kwa ajili ya dhambi au ukaidi wakienda kwenye hekalu na kuomba kusamehewa makosa yao (maana hakuna mtu asiyekosa) basi BWANA awasamehe.

Sulemani akamaliza ombi lake na kusema macho ya Mungu yawafungukie, na masikio yake yawasikilize kwa yale waombayo. “Sasa Ee BWANA, Mungu, uondoke uende kwenye raha yako, wewe na sanduku la nguvu zako, makuhani wako, Ee BWANA Mungu, wavikwe wokovu, watakatifu wako na wakushangilie mapema. Usirudishe uso wako, uzikumbuke fadhili za Daudi mtumishi wako.” Alipomaliza kuomba, moto ukashuka kutoka mbinguni ukateketeza dhabihu, utukufu wa BWANA ukaijaza nyumba, wala makuhani hawakuweza kuingia nyumbani mwa BWANA kwa ule utukufu. Wakatazama watu wote uliposhuka ule ukutufu, wakasujudu kifudifudi hata sakafuni, wakamshukuru BWANA na kusema “ni mwema, kwa maana fadhili zake ni za milele.” Ndipo mfalme akatoa dhabihu za ngombe 22,000 na kondoo 120,000 na wakamaliza kuweka wakfu nyumba ya BWANA. Wakafanya sherehe ya siku saba. Siku ya 14 akawaruhusu watu waende hemani kwao wakifurahi na kuchangamka mioyoni kwa wema wote wa BWANA aliomfanyia Daudi, Sulemani, na Israeli watu wake.

Hekalu lilikuwa ndiyo kiini cha mambo yote yaliyoendelea katika Israeli. Kilikuwa ndio kitovu cha mambo. Sanduku la ushuhuda lilikuwa ndio alama kuu ya utukufu na uwepo wa Mungu. Liliitwa sanduku la agano kwa vile kulikuwa na Sheria au Agano.

Kitu kimoja cha kutia makini, ni, wakati Sulemani akijenga hekalu, hakuingia katika shida ya dhambi. Bali aliponza kujifanyia kazi zake ndipo shida ikaanza.

Sulemani akaweka zamu za kutumika makuhani na walawi, kulinda, kuhudumu kwa zamu kila siku. Kama alivyoamuru baba yake Daudi. Kuhusu kujiosha kabla ya kuhudumu kwenye karai kubwa. Kristo alipokufa, watu Wake walitakaswa mara moja kwa wakati wote kwa damu Yake iliyomwagika msalabani. Hatuhitaji tena kuoshwa kwa maji ili kuja mbele za Mungu kama walivyofanya hekaluni siku zile, kwa sababu Kristo “amefanya utakaso wa dhambi” (Waebrania 1:3). Sasa

tunaweza “kukikaribia kiti cha neema kwa ujasiri” (Waebrania 4:16), tukiwa na uhakika kwamba tunakubalika Kwake kwa sababu sisi ni safi kupitia Yeye Masihi.

Sulemani alianza kujenga nyumba yake, hakutaka mke wake Mmisri akae karibu na hekalu “Mke wangu hatakaa nyumbani mwa Daudi mfalme wa Israeli, kwa kuwa ni patakatifu, mahali palipofika sanduku la BWANA.” Ila alijenga madhabahu nje ya ukumbi wake. 2 Mambo ya Nyakati 8:11.

La muhimu zaidi leo ni kujua sisi ni hekalu ya Bwana lililo katika ujenzi “Mwanadamu ni kazi ya Mungu, yeye ni hekalu la Mungu, kazi ya Bwana ambayo ni kito cha thamani, kazi iliyoumbwa kwa kusudi la juu na takatifu; na katika kila sehemu ya hekalu la kibinadamu Mungu anatamani kuandika sheria Yake. Kila neva na misuli, kila majaliwa ya kiakili na kimwili, yanapaswa kuwekwa safi. Miili yetu ipo katika ujenzi leo, ili tabia zetu zifanane Naye.

Mungu anapanga kwamba mwili uwe hekalu la Roho Wake. Ni shida ikiwa tunachafua miili yetu, au kujidhuru wenyewe kwa mawazo machafu, pombe, sigara, chakula kibovu, michezo isiyofaa, kiburi nk.

Kristo alikufa ili sura ya kimaadili ya Mungu iweze kurejeshwa katika ubinadamu, ili wanaume na wanawake wawe washiriki wa tabia ya Bwana, wakiwa wameepuka uharibifu uliomo duniani kwa njia ya tamaa. Hatupaswi kutumia nguvu zozote za nafsi zetu kwa ajili ya kujitosheleza wenyewe na ubinafsi; kwa maana nguvu zetu zote ni Zake Mungu, na zinapasa kutumika kwa utukufu Wake.

“Tumeumbwa kwa jinsi ya ajabu na ya kutisha.” Kazi ya Mungu inapaswa kulindwa, ili ulimwengu wa mbinguni na jamii ya waasi yaani binadamu ipate kuona kwamba wanaume na wanawake ni mahekalu ya Mungu aliye hai.

Ukamilifu wa tabia ambayo Mungu anaitaka ni kuweka mwili wetu mzima kama hekalu la kukaa Roho Mtakatifu. Bwana anahitaji huduma ya nafsi yote. Sio nusu nusu. Anatamani wasichana na wavulana wawe vile ambavyo amewawezesha kuwa. Haitoshi kwa sehemu tu ya mwili wa binadamu kutumika. Kristo alipokufa, watu Wake walitakaswa mara moja kwa wakati wote kwa damu Yake iliyomwagika msalabani. Hatuhitaji tena kuoshwa kiibada kwa maji ili kuja mbele za Mungu, kwa sababu Kristo “amefanya utakaso wa dhambi” (Waebrania 1:3). Hivyo sasa tunaweza “kukikaribia kiti cha neema kwa ujasiri”

Tuwe majasiri, na tushinde kila mazoea ambayo yanaharibu hekalu la roho. Tumtegemee Mungu kabisa, na imani yetu itaimarishwa kwa kuamini, ingawa hatuwezi kuona kusudi la Mungu katika kushughulika Kwake nasi, au matokeo ya shughuli hii ya ujenzi wa hekalu la miili yetu, ila tutaiona hivi karibuni.

“Makuhani Walawi walipaswa kujiosha kila mara ili kujitayarisha kwa ajili ya uwepo wa Mungu Mtakatifu, lakini Yesu Kristo alitimiza Sheria yote (Mathayo 5:17). Kristo alipokufa mara moja tu watu Wake walitakaswa kwa damu Yake iliyomwagika msalabani. Hatuhitaji tena kuoshwa kiibada kwa maji ili kuja mbele

za Mungu, kwa sababu Kristo "amefanya utakaso wa dhambi" (Waebrania 1:3). Sasa tunaweza "kukikaribia kiti cha neema kwa ujasiri" (Waebrania 4:16), tukiwa na uhakika kwamba tunakubalika Kwake kwa sababu sisi ni safi kiroho, kimwili, kiakili, kiuchumi, na hata kijamii"

*"Tumeungana katika maombi ya dhati karibu na vitanda vya wagonjwa waume, na wake, na watoto, nasi tumehisi kuwa walirudishwa kwetu kutoka katika kifo kama jibu la maombi yetu ya dhati. Katika maombi haya tulifikiri lazima tuwe na mtazamo chanya, na ikiwa tuna imani, ni lazima tuombe kwaajili ya uhai tu. Hatukuthubutu kusema, "Ikiwa itamtukuza MUNGU," tukiogopa kuwa ingekuwa sawa na kuwa na shaka. Tumewaangalia kwa wasiwasi wale ambao wamerudishwa kwetu kama wale waliotoka kifoni. Tumeona baadhi ya hawa, haswa vijana, wakirejeshewa afya, nao wakamsahau MUNGU, wakawa wenye tabia mbaya maishani, wakisababisha huzuni na uchungu kwa wazazi na marafiki, na wamekuwa aibu kwa wale ambao waliogopa kuomba mapenzi ya Mungu yatimizwe. Waliishi kwa kutomheshimu na kumtukuza MUNGU, bali kumlaani kwa maisha yao ya uovu.

---

Somo gani umejifunza hapa? Kwa nini Sanduku la agano lilikuwa muhimu sana? Moto ulitoka wapi? Sulemani aliomba mambo gani saba? Kwa nini Sulemani hakutaka kumleta mke wake karibu na Hekalu? Hekalu la Mungu pia ni miili yetu hata leo, Je! Unaweza kuelezea jinsi ya kutunza hili hekalu? Hali ya kiroho ya washiriki ni jambo la muhimu zaidi kuliko hekalu lenye majengo mazuri, unaweza kuelezea jambo hili?

**SIKU YA 112**
**(Aprili 21)**

# Jibu la BWANA kwa Sulemani

**- 1 Wafalme na 2 Mambo ya Nyakati 7 na 9**



Bwana akamtokea Sulemani usiku na akamwambia, "Nimesikia uliyoyaomba, na mahali hapa nimejichagulia kuwa nyumba ya dhabihu. Nikizifunga mbingu isiwe mvua, tena nikiamuru nzige kula nchi, au nikiwapelekea watu wangu tauni; ikiwa watu Wangu, walioitwa kwa Jina Langu, watajinyenyekeza, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao." BWANA akasema macho Yake yatafumbuka na masikio Yake yatasikiliza maombi ya watu waombao hekaluni. Akasema amelichagua hekalu hilo na kulitakasa, ili kwamba jina lake lipate kuwako milele, kama akienda mbele zake kama baba yake Daudi na kufanya alivyoamuru kwa kushika sheria, na amri zake. Lakini wakigeuka na kuabudu miungu mingine ataifanya nchi yao kuwa tukano katika watu wote, na kila mtu atakayeona akipita atapata mshangao na kusema, "mbona BWANA ameitendea hivi nchi hii na nyumba hii" na watu watajibu "Kwa sababu walimwacha BWANA, Mungu wa baba zao, aliyewaleta kutoka nchi ya Misri, wakashikamana na miungu mingine, wakaiabudu, na kuitumikia; kwa hiyo ameyaleta mabaya haya yote juu yao. Hata leo BWANA yuko tayari kusikia maombi yetu. Kama tukitubu na kumrudia, Yeye naye atatusamehe na kuiponya nchi yetu.

Sura ya 1 Nyakati 23 hudhihirisha kwamba Mungu aliwaagiza Walawi – wale waliotunza hekalu la kale la Kiyahudi na huduma Zake – kusimama katika uwepo Wake wakiinua sauti zao katika kushukuru na kumsifu kila asubuhi na jioni. Zoezi hili la ibada chimbuko lake ni katika amri nyingine ambayo Mungu alimpatia Musa alipowaagiza Waisraeli akisema "wanifanyie Patakatifu; ili nipate kukaa kati yao" (Kutoka 25:8). Mungu aliagiza zaidi kuwa, "Mwana-kondoo mmoja utamchinja asubuhi; na mwana-kondoo wa pili utamchinja jioni" (Kutoka 29:39). Ikiwa maisha yako ya maombi yamepoteza hadhi yake, mwombe Mungu sasa aweze kufanya upya msimamo wako kwa ibada ya asubuhi na jioni leo, kwa kuomba na kusoma Maandiko.

Wengi walisikia ukuu na hekima ya Sulemani nao wakaja kumtembelea na

kuzungumza naye kutafuta mashauri au kuzuru na kuona maajabu hayo. Utajiri na nguvu Mungu anazotupatia inapasa ziwe ushuhuda kwa ukuu wa Mungu na siyo kutujengea kiburi au kutuingiza dhambini. Basi malkia wa Sheba naye akaenda kumtembelea Sulemani ili amjaribu kwa maswali ya fumbo huko Yerusalemu. Akaja na wafuasi au wafanyakazi wengi, ngamia wachukuao manukato, na dhahabu na vito vya thamani.

Alipofika kwa Sulemani alimwambia mambo yaliyo moyoni mwake, naye Sulemani akamfumbulia maswali yake yote, wala halikuwako neno alilofichwa Sulemani asimwambie. Naye alipoona hekima ya Sulemani na nyumba aliyoijenga, na vyakula vyake mezani na watumsihi wake na usimamizi wao, mavazi, wanyweshaji, ghorofa ya kupandia hekaluni, roho yake ilizimia. Akamwambia mfalme, amesikia habari zake akiwa kwao, lakini hakusadiki kwamba ni maneno ya kweli, "hata nilipokuja na kuona kwa macho yangu, wala tazama ukuu wa hekima yako sikuambiwa hata nusu, wewe umezidi kuliko habari nilizosimuliwa. Heri watu wako na heri watumishi wako wasimamao mbele zako wakisikia hekima yako siku zote. Na ahimidiwe BWANA, Mungu wako aliyependezwa nawe, ili akuweke juu ya kiti chake cha enzi." Akampa mfalme talanta za dhahabu, manukato mengi sana, na vito vya thamani. Hakuna aliyeleta manukato mengi kama malkia wa Sheba. Naye Sulemani akampatia Malkia wa Sheba zawadi nyingi, kuliko malkia alizoleta na haja zake zote. Alipewa kila alilotaka, naye akarudi katika nchi yake na watumishi wake baada ya mwaka? Malkia wa Sheba alikuwa mwaminifu kwa Mungu kuliko Wayahudi wengi, maana Yesu alisema, "Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani." Hakuna kitabu kikuu cha Historia ya dunia, kama Biblia, mengi yanazidi kuvumbuliwa. Ikiwa sasa hivi huelewi jambo fulani, mwombe Mungu, kuna siku utafunuliwa na kuona kwamba hakuna kinachopingana na Biblia.

Mungu alimchagua Sulemani akiwa mchanga bado na mwororo katika kazi kubwa atakayomfanyia. Hata watu walikuwa wamechangia kwa kiasi kikubwa pia ujenzi wa Hekalu. Watu walitoa kwa hiari yao wenyewe, kwa sababu ya ukamilifu wa mioyo yao, nao wakafurahi kwa furaha kuu. Walitoa mali na hata talanta zao. Hata leo kutoa ni jambo la furaha, na lina baraka nyingi, hasa katika kusaidia wenye mahitaji na kazi ya Mungu hekaluni kama alivyofanya mfalme Daudi na Sulemani. Maana utajiri, kuwezeshwa, heshima na baraka zinatoka kwa Mungu. Daudi alisema "Mimi ni nani na watu wangu ni nani, hata tuweze kutoa kwa hiari hivi? Kwani vitu vyote vyatoka kwako na katika vitu vyako mwenyewe tumekutolea. Mungu anajaribu mioyo yetu na anapendezwa na unyofu. Bwana alimtukuza Sulemani machoni pa Israeli, na akampa fahari ya kifalme ya kuzidi baba yake au mfalme yeyote wa Israeli.

Katika kitabu cha 1 Mambo ya Nyakati 4, tunamwona kijana Yabesi, wa kabila la Yuda, ambaye mama yake alimzaa kwa huzuni, ila yeye alikuwa mtu mwungwana kuliko ndugu zake. Huyu alimlilia Mungu na kusema, Lau kama ungenibarikia kwelikweli, na kunizidishia milki yangu, na mkono wako ungekuwa pamoja nami,

nawe ungenilinda na uovu, ili usiwe kwa huzuni yangu. Na Mungu akamjalia haja ya moyo wake aliyoiomba. Hata na leo sisi Mungu anatujalia haja za mioyo yetu.

Zama zile walijenga hekalu moja, siku hizi tuna mamilioni ya makanisa kila mahali. Wanapoanza kujenga kanisa, japo huna kazi ya kuajiriwa, uwe mmojawapo wa wale wanaochangia. Ni vyema ujenzi usiwe na madeni unapoenda kumalizika. Mwombe Mungu akupatie kitu cha kutoa ili kujenga kanisa, ni baraka kubwa kujenga nyumba ya MFALME WA WAFALME.

Hata leo, hebu tuwe kama Sulemani, kumchagua Mungu kuwa Baba yetu, nasi tuwe wanawe, ili atuweke imara milele. Watoto tuwe hodari, na wenye moyo mkuu, tukatende na kumpendeza Mungu. Tusiogope wala tusifadhaike, kwa kuwa BWANA Mungu yu pamoja nasi, naye hatatupungukia wala kutuacha, hata atakaporudi mara ya pili kutuchukua.

Kila mwaka Sulemani akapata zawadi toka nchi mbali mbali.

*Katika kuwaombea wagonjwa, tunapaswa kuomba kwamba ikiwa ni mapenzi ya MUNGU basi waponywe wawe na afya; lakini ikiwa vinginevyo kwamba awape neema Yake ya kuwafariji, na uwepo Wake uwadumishe katika mateso yao. Wengi wanaopaswa kuweka nyumba zao sawa, yaani katika mpangilio, hupuuza kufanya hivyo wakati wana tumaini kwamba watainuliwa kiafya katika kujibiwa maombi. Wakichochewa na tumaini la uwongo, hawahisi hitaji la kutoa maneno ya mawaidha na ushauri kwa watoto wao, wazazi, au marafiki, na ni bahati mbaya sana. Wakikubali uhakikisho wa kwamba wangeponywa wakati wa kuombewa, hawathubutu kutaja jinsi mali zao zitakaavyogawiwa, jinsi familia yao inavyopaswa kutunzwa, au kueleza matamanio yoyote kuhusu mambo ambayo wangezungumza ikiwa walidhani wangeondolewa na kifo. Kwa njia hii majanga huletwa kwenye familia na marafiki; kwa maana mambo mengi ambayo yanapaswa kueleweka yameachwa bila kutajwa au kuzungumziwa, kwa sababu wanaogopa kuwa kujieleza juu ya mambo haya itakuwa ni kuikana imani yao. Wakiamini watainuliwa kiafya kwasababu ya maombi, wanashindwa kutumia njia au kanuni za afya, au usafi ambazo ziko katika uwezo wao, wakihofia kuwa kutenda hilo ni kuikana imani yao.

---

Mungu alijibuje ombi la Sulemani? Watu walitoa nini na Daudi alitoa nini ili kujenga hekalu? Kwa nini Malkia wa Ethiopia alikuja kumtembelea Sulemani? Alileta zawadi gani? Yabesi alimwomba Mungu nini?

**SIKU YA 113**
**(Aprili 22)**

# Wimbo Ulio Bora au Wimbo wa Sulemani




Kitabu cha wimbo ulio bora anazungumza kuhusu upendo kati ya mwanamke na mwanamume. Upendo huu uwe ndani ya ndoa na si nje, ndilo agizo la Mungu. Upendo wa Mungu kwa kanisa lake, unalinganishwa na upendo wa mume kwa mke. Apataye mke au mume mwema, apewa na BWANA naye apata kitu kizuri. Huzuni itakuwa nyingi endapo mke au mume atakuwa ni mkatili au asiyempenda Mungu. Mithali 5, 6 na 7 zinazungumza kuhusu mwanamke mgeni au mbaya, kinyume cha mwanamke huyu ni Mithali 31 ambayo inazungumzia mwanamke bora, mbele za Mungu, kwa mume wake na watoto pia. Kila msichana na mvulana asome mausia ya Sulemani ili asirudie makosa yake. Hawa alipojua wema na uovu, huzuni iliongezeka, akajikuta hajui kitu na yuko tupu. Wanawake walimtoa Sulemani kwa Mungu, aliyekuwa chanzo cha hekima yake. Kumcha Mungu ndiyo chanzo cha hekima. Anatukumbusha kutojipatia wake/waume wa namna hii. Hata leo, japo u mtoto, bado unaweza kumwomba Mungu akusaidie ili wakati ukifika, uweze kuoa au kuolewa na mtu anayemcha Mungu. Maana utajichoma kwa maumivu mengi ukipata kafiri au mwovu yoyote mnayekutana naye. Wengi wamejiunga na makundi ya marafiki wabaya wakififikiri watakimbia wanapotaka kuachana na hawa. Kama Sulemani mwenye hekima nyingi, alishindwa kuwakimbia wanawake hawa waovu, kwa vile aliwakaribisha kwake, akazungumza nao na kufanya urafiki nao. Je, sisi tusio na hekima kama yeye tutapona kweli tukiwa na marafiki wanaoabudu mambo mengine, eti, tunafikiri tutakimbia tukitaka?

Upendo na neema ya Mungu ni kuu na za ajabu mno, zilimrudisha akutubu. Wengine hawana nafasi kama yake, wakipotea ndio mwisho wao. Hata mke wake wa kwanza,

binti wa Farao wa Misri kwa neema aliamua kumwabudu Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Na hii ingekuwa ishara aache kuoa wanawake wageni waliotoka nchi ambazo wanaabudu miungu mingine. Kwa wafalme hawa kuwa na wake na watoto wengi, kulitimiza unabii wa Samweli wa wafalme kuwafanya watumishi wa mji wake na kuwapa huzuni raia zake.

Wimbo wa Sulemani ni mojawapo kati ya zile 1005 alizoandika akiwa kijana. Wengi wamesita kukisoma wakifikiri ni mambo yasiyovuviwa. Hii si kweli, kwani Mungu ndiye aliyeanzisha ndoa, au mahusiano ya ndoa kati ya mume na mke. Pengine kama kwenye kitabu kile cha Esta hakina Neno 'Mungu', ila kimevuviwa na Roho wa Mungu. "Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu makosa yao na kwa kuwaongoza, na kuwaadabisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."

Wimbo huu unaanza na uchumba, kabla ya arusi. Mshulami ndiye msichana anayetaka kuwa karibu na mchumba wake, ila anashauri kutoharakisha, atoe muda ili upendo ukue wenyewe. Anawapa mausia wasichana wenzake wengine "wasiyachochee mapenzi mpaka wakati wake ufike." Mwanamume ambaye ni mfalme Sulemani, anamsifu Mshulami, na hii inapunguza hofu za msichana kwamba 'uzuri wake hautoshi.' Mshulami anaota ndoto kwamba amempoteza mchumba wake Sulemani, na akamtafuta mji mzima walinzi wakajiunga kumsaidia. Siku ya harusi, bwana harusi anamsifu mke wake, wanashirikiana na kuwa mwili mmoja. Ndoa inavyoendelea wanafika pagumu, kwa ndoto Mshulami anagombana na mumewe na mume anaondoka. Anamtafuta tena mji wote, safari hii walinzi wakimwona wanampiga, ndoto inaishia na wapenzi wanaungana tena.

Upendo kati ya mke na mume si kitu cha wakati wa giza, siri au vificho. Mfano, kumshika mkono, kuzungumza maneno matamu au ya kutia moyo, n.k. Watu hujua kidogo kama kemia ipo kwa wapendanao au ni historia tu imebaki. Mahaba yaendelee baada ya ndoa, na yapaswa yawe mengi zaidi ya kabla ya ndoa.

Upendo kati ya mume na mke, ni mpango ambao Mungu aliweka, wakati wa uumbaji. "Mpendwa wangu, ni wangu na mimi ni wake," Wimbo 2:1. Huu si wimbo wa kawaida, umewekwa kimashairi yaliyokusanywa ya mwanamume akizungumza na msichana. Yanaonesha ni vijana bado, na ni mabikira bado. Yanaelezea jinsi mwanamume anavyosifia upendo na tabia ya msichana na msichana kadhalika. "Tazama u mzuri, mpenzi wangu, u mzuri macho yako ni kama ya hua." Wapenzi hawa wamependana na wazazi wao wanajulishwa, si kitu cha siri. Mahaba ni sehemu ya maisha ambayo Mungu anataka mume na mke wawe nayo, na sehemu yake salama ni katika ndoa tu. "Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake na kuambatana na mke wake nao watakuwa mwili mmoja, alichokiunganisha Mungu mwanadamu asikitenganishe." Wimbo unaanza kabla ya harusi, wakati wa uchumba na kuendelea mpaka kutambulishana na kuishi pamoja. Tukitaka furaha na mapenzi ya kweli ya ndoa, sharti tufuate mpango wa Mungu, na kupitia hatua zinazofaa na si kufanya uasherati na kuchafua miili yetu. "Nawasihi binti za Yerusalemu… Msiyachochee mapenzi wala kuyaamsha hata yatakapoona vyema yenyewe." Sulemani anakiri kuwa "upendo una nguvu kuliko mauti…maji mengi

hayawezi kuuzimisha upendo."

Tunaishi wakati ambao upendo kati ya watu na hata mume na mke unapungua na talaka zinazidi kuongezeka, na hivyo maelekezo haya ni mazuri ili kusaidia upendo wa mume na mke kuwa wa kweli na usio na kifani. Na kwamba Mungu ana upendo usio na kikomo au masharti kwetu, yaani, agape. Mtu amjue vizuri mke/mume ili kutoa muda wa kujenga mahusiano. Mke/mume wajifunze maneno mazuri na matamu ya kutiana moyo na siyo kukosoana kila wakati. Mume/mke afanye yote yaliyo kwenye uwezo wake ili kumfurahisha mwingine, na kuonesha kujali kwake na kuwajibika kwa mwenzake. Mume/mke wanapaswa kuzifanya nadhiri na maagano yao kuwa mapya kila siku na kuzirejea. Wasifikiri talaka ni suluhisho la shida zao. Mungu anataka waishi kwa amani na usalama. Mume/mke wajifunze kumsikiliza mwenzi wao na si wao tu wasikilizwe.

Biblia inasema, "Enyi waume wapendeni wake zenu kama Kristo naye alivyolipenda kanisa na akajitoa kwa ajili yake." Na wake, "wawatii waume zao kama kumtii BWANA, kwa maana mume ni kichwa cha mkewe kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa, naye ni Mwokozi wa mwili." Kitabu hiki kinaweza kutumika kuelezea upendo wa Mungu kwetu sisi pia. Au upendo wa Mungu kwa kanisa lake.

"Mpenzi wangu u mzuri pia wala ndani yako hamna ila". Linganisha Wimbo Ulio Bora 4:7 na Waefeso 5:27.

"Mambo yanayosaidia ndoa kuwa bora ni pamoja na kumtakia mwenzi mema na si kumwazia mabaya. Kusali pamoja, kuendelea kuchumbiana, kukumbuka ni Mungu aliyewaunganisha, kulinda mawazo yasitembee huku na kule, kutolala na hasira, kumweka Mungu kuwa kiini cha maisha, kukubaliana kwamba talaka si jibu, kutokosoana na kusakamana, kuwa na kiasi, kuheshimu haki za mtu na kumwachia mwenzi nafasi ya faragha, kuangalia mambo ya usafi, mipangilio na majukumu, kujua kutumia fedha kwa hekima, na kuwa huru kuzungumza pamoja na kushauriana, kuheshimiana na kupendana. Ndoa ilitolewa idumu mpaka kifo kitenganishe watu. Nakazia, kijana anapaswa kuwa makini sana anapochagua mchumba. Awe ni mtu anayempenda Mungu, mwenye tabia ya kufaa na ambaye anachukuliana vyema, kusiwe na tofauti sana ya tabia au malengo kiasi kwamba mmoja akawa na huzuni kumtimizia mahitaji ya mwingine. Yote yafanyike kwa kusali sana, kupata ushauri kwa watu wazima wampendao Mungu na kusoma Maandiko. Hakuna mtu mkamilifu duniani, ila tabia fulani kama ulevi, uongo, usengenyaji, kukosa uaminifu, wivu, kiburi, vinafanya ndoa iwe na masikitiko mengi. Kwa vile mara zingine kijana hawezi kumfahamu mchumba wake sana, basi azidi kumwomba Mungu ili amwoneshe la kufanya kama Eliezeri, na siyo kujitafutia mtu na kumfahamisha Mungu kwa kusema, "nimeshachagua mwenyewe nibariki na huyu."

Ndoa iliyoandikwa kwenye Neno la Mungu ni kati ya mwanamume na mwanamke, na inapaswa kufungwa kisheria kwenye nyumba ya ibada. Ndoa inaweza kufanywa kuwa mpya ili kama ya Sulemani na Mshulami kwa kufanya haya pamoja: Kushangiliana, kusifiana, kuandikiana, kucheka, kutatua matatizo, kucheza pamoja,

kubarizi, kuongea, kurejea nadhiri za ndoa, kumsikiliza mwenzi, kutochoka kutenda wema, kusafiri pamoja, kufanya kazi pamoja, kuoneshana huruma na upole.

*"Tumeungana katika maombi ya dhati karibu na vitanda vya wagonjwa waume, na wake, na watoto, nasi tumehisi kuwa walirudishwa kwetu kutoka katika kifo kama jibu la maombi yetu ya dhati. Katika maombi haya tulifikiri lazima tuwe na mtazamo chanya, na ikiwa tuna imani, ni lazima tuombe kwaajili ya uhai tu. Hatukuthubutu kusema, "Ikiwa itamtukuza MUNGU," tukiogopa kuwa ingekuwa sawa na kuwa na shaka. Tumewaangalia kwa wasiwasi wale ambao wamerudishwa kwetu kama wale waliotoka kifoni. Tumeona baadhi ya hawa, haswa vijana, wakirejeshewa afya, nao wakamsahau MUNGU, wakawa wenye tabia mbaya maishani, wakisababisha huzuni na uchungu kwa wazazi na marafiki, na wamekuwa aibu kwa wale ambao waliogopa kuomba mapenzi ya Mungu yatimizwe. Waliishi kwa kutomheshimu na kumtukuza MUNGU, bali kumlaani kwa maisha yao ya uovu.

---

Ni nani mwanzilishi wa ndoa? Ndoa inawezaje kufanywa upya? Kwa nini mahaba ni muhimu kwenye ndoa zote? Kwa nini wanaume wanapaswa kuwapenda wake zao? Mungu ni mfano wa nani kwenye ndoa, na mke ni mfano wa nani? Ni mambo gani yanaweza kuboresha na kufanya ndoa iwe na furaha? Mshulami anashaurije wasichana na wote ambao hawajakomaa kiumri, kiakili na kiuchumi, anaposema "kusiwe na haraka ya kuchochea mapenzi mpaka umri ufike"?

**SIKU YA 114**
**(Aprili 23)**

# Sulemani Amwacha Mungu

**- 1 Wafalme 11**

Sulemani alikuwa mtu anayempenda Mungu kwa namna ya pekee tangu utotoni. Hakuwa mtoto wa kwanza wa urithi, kwani Amnoni ndiye alikuwa wa kwanza, na hata baada ya kufa, Amnoni, na Absalomu, ilikuwa Danieli mwana wa Abigaili au Adonia watawale, lakini Mungu alimchagua Sulemani. Baba yake hakusita kumwachia ufalme na kazi ya kujenga hekalu japo alimwona bado yu mdogo. Alisema, "Mwanangu akali mchanga na mwororo, na nyumba ya BWANA atakayoijenga haina budi kuwa nzuri mno, yenye sifa na yenye fahari katika nchi zote." Kisha akaweka akiba tele kabla hajafa. Akambariki afanikiwe, na BWANA ampe busara na akili na aishike torati ya BWANA, ndipo atakapofanikiwa, akiangalia na kutenda amri na hukumu BWANA alizomwagiza Musa.

Basi mfalme Sulemani alianguka kwa kupenda wanawake wengi wageni, "Wamoabi, Waamoni, Waedomi, Wasidoni, Wahiti, na wa mataifa BWANA aliyowaambia wana wa Israeli wasioe wala kuingia kwao, na wao wasiingie kwenu." "Kwa vile wataigeuza mioyo yao na kuifuata miungu yao." Sulemani aliambatana na wanawake hawa na kuwapenda, akawa na wake 700 na masuria 300. Jambo la ajabu kabisa, kwani hata mke mmoja kukaa naye kunahitaji hekima kubwa. Alianza vyema, akiwa mtoto, na mwenye hekima na kumcha Mungu; alipokuwa mzee akageuzwa moyo wake, afuate miungu mingine, wala moyo wake haukuwa mkamilifu kwa BWANA, Mungu wake, kama moyo wa Daudi, baba yake. Alianza kumfuata Ashtorethi mungu mke wa Wasidoni, na Milkomu, chukizo la Waamoni, mungu ambaye alifanya watu watoe watoto wao wadogo kama sadaka za kuteketezwa. Sulemani akafanya mabaya machoni pa BWANA, akaacha utimilifu na akamjengea Kemoshi, chukizo la Wamoabi mahali pa juu pa kutoa sadaka kwa miungu, na Moleki chukizo la wana wa Amoni. Akafanya ibada hizi za miungu ya machukizo na wake zake wageni, akifukiza uvumba na kutolea miungu yao dhabihu. Soma zaidi kwenye mtandao wa google "Lessons from the life of Solomon-Review and Herald."

BWANA akamghadhibikia Sulemani, kwa sababu moyo wake umegeuka na amemwacha BWANA, Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Israeli. Akampa karipio asifuate miungu hiyo naye hakusikia aliyoamriwa. BWANA akasema kwa vile hakuyashika aliyoamuru, "nitararua ufalme usiwe wako, nami nitampa mtumishi wako." Ila akasema hatafanya hilo katika siku zake akitawala, kwa ajili ya ahadi aliyompa Daudi. Akasema kabila la Yuda atapewa mwanawe, ila makabila mengine, mtu mwingine atayachukua na kutawala. Wanawake walimchukulia Sulemani moyo wake na hekima, kisha upendo wake kwa Mungu aliyemtoa mbali ukaanza kutoweka.

BWANA akamwondokeshea Sulemani adui, Hadadi Mwedomi, na kisha Rezoni na

hata Yeroboamu. Mungu akamtuma Nabii Ahiya kwenda kwa Yeroboamu, naye alikutana naye njiani na kumpa ujumbe, kwa kurarua vazi lake jipya vipande 12 na kumwambia Yeroboamu atwae vipande kumi. Akampa tafsiri kuwa ni kuraruliwa kwa utawala wa Sulemani na kumpa Yeroboamu kabila kumi, kwa ajili ya kumwacha Mungu na kuabudu miungu mingine. Sulemani aliacha njia ya Mungu na kutenda yaliyo mema machoni pake mwenyewe, akaacha hukumu na sheria za Mungu. Giza likawa limeingia katika Israeli. Kwa sababu ya kupenda wanawake wengi, Sulemani alimwacha BWANA. Mali, kiburi na kupenda wanawake imekuwa ni sababu ya kuanguka kwa wengi wanaompenda Mungu wanapopata nafasi ya kuongoza watu. Watu wanaoongozwa wanaona mifano hii miovu, na wengi pia wanachukuliwa na wimbi hilo. Sulemani alifanya mambo yote kwa ukubwa, iwe ni kujenga hekalu, kuoa wake wengi nk. Unaweza kupiga picha mtu akija kanisani na wanawake 1000 na watoto 2000, Je, wanaweza kupata mahali pa kukaa, Je, meza ya chakula shule na mambo mengine, gharama zake zilikuwaje kwa raia wake? Yeye alikuwa na hekima kuliko mtu yeyote katika ulimwengu uliojulikana wakati huo. Alikuwa na kila kitu! Basi kama alijiruhusu kukengeushwa na mambo ya mahusiano ya karibu na wale wasio waamini, sisi tuna hatari kubwa kiasi gani? Sisi ambao tunaishi katika ulimwengu wa mitandao, simu za mikono na uchafu mwingi zaidi unaoenea kwa media kuliko wakati wake, yatupasa tunyate kwa tahadhari zaidi. Tudumu katika maombi na kuzikimbia tamaa za dunia na ushawishi wake! Tuuweke msalaba karibu. Ombi ni kuwa Eh, Bwana unifiche chini ya mbawa zako. Nilinde kutokana na ushawishi mbaya na vikengeusho. Nisaidie nisipoteze upendo wangu wa kwanza Kwako. Narudia tena, "ni vigumu sana kuelewa jinsi mtu mwenye hekima kama huyo, ambaye alizungumza na Mungu na kupokea zawadi Zake zote za kiakili kutoka kwa Mungu, angeweza kugeuka kutoka kwa sheria Zake kiasi hicho. Ufunguo wa haya yote ni kwamba "alipenda wanawake wageni", yaani wasiomwamini Mungu wa mbinguni. Mwanamke au mwanamume mmoja tu, anaweza kumfanya mtu awe mpotevu. Tumeona vijana wengi wanaopuuza ushauri wa wazazi na wachungaji wao na kushirikiana na wanaume na wanawake wasiompenda Bwana. Mengi ya mahusiano haya yamekuwa mabaya! Mungu ambaye alijivunia sana Sulemani na kumpa hekima nyingi alihuzunika moyoni.

Kwa kuendelea na sura yetu, tunaona Sulemani aliposikia kuwa Yeroboamu atapewa sehemu ya ufalme, yeye akataka kumwua. Yeroboamu aliposikia alikimbia na kwenda Misri, hata Sulemani alipokufa. Sulemani alitawala Israeli miaka 40.

*"Hatutengenezi njia tena wala kutafuta kumleta Bwana katika matamanio yetu. Ikiwa maisha ya wagonjwa yanaweza kumtukuza Yeye, tunaomba kwamba waishi, hata hivyo, si kama sisi tutakavyo bali kama Yeye atakavyo. Imani yetu inaweza kuwa imara, na ya uhakika kwa kuyakabidhi matamanio yetu kwa MUNGU Mwenye hekima yote, na, bila wasiwasi au homa, na kwa ujasiri mkamilifu, tukimwamini Yeye. Tunayo ahadi. Tunajua kwamba Yeye hutusikia ikiwa tunaomba kulingana na mapenzi Yake.

---


Anguko la Sulemani lililetwa na nini? Kwa nini tunasema giza liliingia katika Israeli? Tunajifunza nini toka kwa Sulemani kuhusu maisha yetu? Sulemani alipewa

mausia gani na babaye? Zamu za makuhani zilisaidiaje?

**SIKU YA 115**
**(Aprili 24)**

# Rehoboamu Mwana wa Sulemani Arithi Yuda, Jinsi ya sisi Kuepuka Majuto

**- 1 Wafalme 12 na 2 Mambo ya Nyakati 9-11**



Sulemani alikuwa na kasoro kama za wafalme wengine kwenye utawala wake, kama ambavyo Mungu alikuwa amesema wafalme watakuwa. Ili kustarehe na kuwa na mambo ya fahari, alitoza watu kodi kubwa mno, watu wa kabila zote za Israeli, kwani alikuwa na watu wengi wakimfanyia kazi, jeshini, kwenye majengo yake na hata nyumbani kwake. Kama alikuwa na wanawake 1000, basi watoto kwa kukadiria walikuwa wengi; hawa wote walitumikiwa, kwa aina mbali mbambali ambazo tunajua watumishi wanatumikia familia zenye uwezo. Watoto walilishwa, vyakula kupikiwa, nguo kufuliwa, nyumba kufagiliwa, mashamba kulimwa, watoto kufundishwa, watoto kuburudishwa, kushugulikia michezo ya watoto, bustani za wanyama na mengineyo. Kabla Sulemani hajatoka madarakani, watu walianza kulilia wingi wa kodi za Sulemani, kwani zilikuwa kongwa zito alilowatwika Israeli. Kodi hizi ziliwaumiza wasiojiweza. Inawezekana hata kafara alizotoa kwa miungu mingine zilikuwa ni mapato ya kodi za watu. Kweli mtawala akimjali Mungu inafanya hata raia wake wamche Mungu. Uongozi unasaidia watu wamjali Mungu au wasimjali.

Mungu alimpelekea ujumbe Yeroboamu, mtumishi wa Sulemani aliyemsaidia kujenga nyumba yake ya kifalme, na kumwambia, endapo atatenda mapenzi yake atakuwa pamoja naye, na atawapa vizazi vyake kutawala. Ufalme wa Sulemani ulikuwa tayari kuanguka na kusambaratika. Kijana wake aliye dhaifu, Rehoboamu alirithi, naye akataka kuendeleza kodi kubwa ya baba yake. Hawakutaka kumtawaza Yerusalemu bali Shekemu.

Kabla ya kutawazwa kwake, Israeli wakiwa Shekemu wakamwambia, "Baba yako alilifanya zito kongwa letu; basi sasa upunguze utumwa mgumu wa baba yako, na kongwa lake zito alilotutwika, nasi tutakutumikia." Akawaambia waende na kurudi siku ya tatu awape jibu. Na Rehoboamu akaomba ushauri kwa wazee ili wampe jibu la lile ombi. Wazee wakamwambia kwamba, kama akikubali kuwa mtumishi wa watu na kuwatumikia na kuwajibu maneno mazuri, watakuwa watumishi wake daima. Rehoboamu akaacha ushauri wa wazee akaenda kuomba ushauri kwa

vijana wa rika lake kuhusu mambo ya kodi nzito aliyotoza baba yake. Vijana hawa wakamwambia awaambie watu kwamba, “Kidole changu cha mwisho ni kinene kuliko kiuno cha baba yangu. Basi kama baba yangu aliwatwika kongwa zito, mimi nitaongeza kongwa lenu. Baba yangu aliwapiga mijeledi, lakini mimi nitawapiga kwa nge.” Basi siku ya tatu watu walipomwendea Rehoboamu, akawapa jibu wale watu kwa ukali, na kuacha shauri jema la wazee. Mfalme hakusikia mashauri mema, na hivyo Mungu alitimiza unabii aliotoa kupitia Ahiya, wa kuugawanya ufalme wa Israeli.

Mungu anataka atubariki lakini mara nyingi tunakosa hekima na kuacha njia zake. Acha atusaidie kuepuka majuto. Kuna njia ambayo inaonekana ni ya hekima machoni pa mtu ila mwisho wake ni majuto.Israeli walipodai kuwa na mfalme kama mataifa mengine, Mungu alionya kwamba kutegemeza utawala wa kifalme kungekuwa kongwa zito kwa watu, na kwamba wanapaswa kubaki kuwa theokrasi, yaani ufalme chini ya Mungu Mwenyewe akiwa Mfalme wao. Lakini walikataa kutii ushauri wa Mungu na kusisitiza kuwa na mfalme. Ili kujua jinsi mzigo ulivyokuwa mzito angalia sentensi hii "hiki ndicho chakula alichokula Sulemani na watu katika jumba lake la kifalme kila siku: lita 5,000 za unga, lita 10,000 za nafaka, ndama 10 wanono ambao walilishwa nafaka, ndama 20 waliokula nyasi kondeni, kondoo 100. aina nyingi za kulungu na ndege wanono. ‘Jiongeze’ kwa kufanya hesabu rahisi! Zidisha vitu hivi kwa siku 30 za mwezi, na kisha miaka arobaini ambayo Sulemani alitawala, unapata picha halisi ya kongwa la raia, lakini walijitakia wenyewe.

Kukataa kwa Rehoboamu kupunguza mzigo huu kuligawanya ufalme kuwa sehemu mbili, ufalme wa kaskazini (Israeli), na ufalme wa kusini (Yuda). Israeli hatimaye ilitoweka kama taifa, na Yuda ilitawaliwa na Babeli, na watu wakafanywa mateka kwa miaka sabini. Tunashauriwa kutosikiliza ushauri wa kipumbavu. Rehoboamu na Yeroboamu walisikiliza shauri la kipumbavu, nalo likaleta uharibifu wa taifa kwa kuasi imani. Watu wanafanya kosa hilo leo pia. Hapa kuna ahadi ya ajabu kutoka kwa BWANA ambayo tunapaswa kuidai kila siku “Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; nitakushauri, jicho langu likikutazama.” Hebu tukubali mwaliko Wake wa ajabu! Unasema nini wewe leo?

*Mungu Hujibu Maombi kwaajili ya Wagonjwa — Hakuna nguvu ya kibinadamu inayoweza kuokoa wagonjwa, lakini, kupitia maombi ya imani, Mponyaji Mkuu ametimiza ahadi Yake kwa wale ambao wameliitia Jina Lake.

---

Sulemani alifanya dhambi gani nzito? Dhambi hii ilitokana na nini? Ufalme wa Sulemani ulikuwa na kasoro gani? Rehoboamu alijibuje watu kwa kutotumia hekima? Je, ni mara zote vijana wanakosa hekima na wazee wanakuwa na hekima?

**SIKU YA 116**
**(Aprili 25)**

# Ufalme wa Israeli Wagawanyika

**- 1 Wafalme 12 na 1 Mambo ya Nyakati 10**

Rehoboamu aliacha kusikiliza ushauri wenye hekima wa wazee, akasikiliza ushauri wa rika zake, kwa anguko lake. Hata leo tuna marafiki na washauri wazuri na wabaya, hivyo tuwe makini ili kuepuka ushauri wa watu wasiomjali Mungu, na kwenda kwa watu wanaomcha Mungu. Misukumo ya rika ikamweka kwenye shida Rehoboamu, na watu wa Israeli wakajua hawana urithi au sehemu katika mwana wa Yese, Daudi. Wakaambizana, kila mtu aende hemani kwake, na kutunza nyumba yake mwenyewe. Basi Rehoboamu akatawala juu ya wana wa Israeli waliokuwa Yuda, na alipompeleka kiongozi wake mjumbe, Adoramu, kwa Israeli, walimpiga mawe akafa. Mfalme alipoona vile alipanda gari lake haraka akimbilie Yerusalemu. Hivyo ndiyo Israeli ilivyoasi juu ya nyumba ya Daudi. Rehoboamu alijenga ngombe na akaweka majemedari na vyakula, mafuta na mvinyo, akiweka ngao na mikuki ili kuifanya Yuda iwe na nguvu nyingi.



The Divided Kingdom,
10th - 6th Century BCE

Kisha Israeli wakasikia kwamba Yeroboamu amerudi toka Misri, nao wakamwita aje kwenye mkutano, na kumfanya awe mfalme juu ya Israeli yote, wala hakuna aliyeshikamana na nyumba ya Daudi ila kabila la Yuda pekee na Benyamini. Rehoboamu akafika Yerusalemu, akakusanya watu wa Yuda na Benyamini 80,000 ili wapigane na Israeli waurudishe ufalme kwake kama mwana wa Sulemani na mjukuu wa Daudi. Lakini Mungu akamtuma Nabii Shemaya kuwaambia Rehoboamu, na Israeli wote waliokuwa Yuda na Benyamini kwamba, "Hamtapanda wala kupigana na ndugu zenu, wana Israeli; rudini kila mtu nyumbani kwake, kwa kuwa jambo hili limetoka kwangu." Wakasikiliza Neno la BWANA na kurudi, wakaenda makwao. Tenganisha majina haya mawili ya wafalme hawa wawili kwani kiasi fulani yalifanana. Mwana wa Sulemani wa kabila la Yuda, jina lake aliitwa Rehoboamu; na yule mtumishi wa Sulemani aliyekimbilia Misri na kisha kuwa mfalme wa makabila 10 ya Israeli, jina lake aliitwa Yeroboamu. Yeroboamu akajenga

Shekemu katika milima ya Efraimu, akakaa huko. Akatoka huko akajenga Penueli. Yeroboamu akasema moyoni mwake, pengine ufalme wake utairudia nyumba ya Daudi, kama watu wataendelea kupanda kwenda Yerusalemu kutoa dhabihu katika nyumba ya BWANA, maana kulikuwa na mahali pamoja pa kuabudia, yaani Yerusalemu tu. Alifikiri kuwa watu wakipanda kuabudu, mioyo yao itamwendea mwana wa Sulemani, bwana wao na kisha wamwue yeye na kumfuata Rehoboamu.

Haikuchukua muda Yeroboamu kuonyesha tabia na uovu wake wa ndani. Hili ndilo kosa alilolifanya Yeroboamu kwani alitengeneza ng'ombe wawili wa dhahabu na kuwaambia watu, "Ni vigumu kwenu kupanda kwenda Yerusalemu; tazama hii ndiyo miungu yenu, enyi Israeli, iliyowapandisha kutoka nchi ya Misri." Akaweka sanamu moja ya ng'ombe huko Betheli na ya pili huko Dani. Na jambo hili likawa dhambi, maana watu walienda kuabudu mbele ya zile sanamu. Kweli uongozi ni kazi kubwa. Siku ukiwa mkubwa na Mungu akakupa uongozi, kila utakapokanyaga, utazame, kama unafanya watu wamwabudu na kumcha Mungu au unafanya watu kuabudu miungu mingine au mambo mengine. Kuna wafalme wawili tu wa kutumikia, Mungu na Shetani, hakuna katikati. Na yeyote ambaye hajafanya maamuzi ya kumcha na kumtumikia Mungu, japo asiseme, lakini atakuwa anamtumikia adui Shetani. Hakuna falme tatu, ni mbili tu.  Yeroboamu akajenga mahali pa kafara juu ya milima na kuchukua watu wasio walawi kuwa makuhani na kuwaamuru kushika sikukuu za mifano fulani isiyo kamili akiwatolea wale ngombe dhabihu kwa makuhani bandia. Basi makuhani Walawi wote walienda Yuda, kule Yerusalemu. Makuhani bandia aliowaweka Yeroboamu walihudumu, akibuni siku alizotaka kama sikukuu, na akaamuru wana wa Israeli washike hizo kwa kwenda madhabahuni  na kufukiza uvumba. Mfalme wa Israeli akaandama watu wacha Mungu, nao wote waliojikaza kumtafuta BWANA."

Hata leo, mataifa, kabila, lugha na jamaa za dunia zina mifano ya ibada bandia zinazofanana kidogo na mpango aliotoa Mungu. Wanatoa kafara, na kusujudu, bali ni za uongo. Ibada hizi si za kweli, ni kinyume na Mungu wa mbinguni. Mungu atusaidie kujua ibada ya kweli kama anavyosema katika Ufunuo 14 "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja. Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:7. Njia ya Mungu iko katika Madhabahu Yake, turudi kule kwa kusoma kutoka 25 na kitabu cha Waebrania.

*Hebu tufanye kama mitume wa Kristo walivyofanya; hebu tufanye maombi kwaajili ya wagonjwa, kwani wapo wengi ambao hawawezi kufaidika na vituo vyetu vya Sanitarium (tiba rahisi). Bwana ataondoa udhaifu katika kujibu maombi.

---

Ni fundisho gani umepata katika siku ya leo? Kwa nini Rehoboamu aliacha kusikiliza ushauri wa wazee? Kwa nini ni vizuri kupata ushauri kwa watu wenye hekima? Kwa nini Rehoboamu aliacha kupigana? Yeroboamu alifanya dhambi gani? Kwa nini alisahau pale Mungu alipomtoa kwenye utumishi na kuwa mfalme?

SIKU YA 117

# Mkono wa Yeroboamu Wapooza

**- 1 Wafalme 13 na 2 Mambo ya Nyakati 13**



Basi akatoka mtu wa Mungu katika Yuda kwa Neno la BWANA, akafika, Betheli. Akamkuta Yeroboamu amesimama penye madhabahu bandia ili afukize uvumba; basi mtu huyo akapiga kelele juu ya madhabahu, kwa Neno la BWANA akasema, "Ee madhabahu, madhabahu, BWANA asema hivi, angalia mtoto atazaliwa katika nyumba ya Daudi, jina lake Yosia; na juu yako atawachinja makuhani wa mahali pa juu, wanaofukiza uvumba juu yako, na mifupa ya watu itateketezwa juu yako. Akatoa ishara siku ile ile, akasema, Hii ndiyo ishara aliyoinena BWANA, Tazama madhabahu itapasuka na majivu yaliyo juu yake yatamwagika."

Mfalme Yeroboamu alipomwona yule mtu anapiga kelele, alinyosha mkono wake akiwaambia watu wamkamate yule mtu wa Mungu. Mkono wa mfalme, ukakauka wala hakuweza kuurudisha kwake tena. Madhabahu ikapasuka, majivu ya madhabahuni yakamwagika, sawasawa na ishara aliyoitoa mtu wa Mungu kwa Neno la BWANA. Basi, mfalme ambaye sasa alikuwa na adabu na hofu, akamsihi yule mtu wa Mungu amsihi BWANA ili arudishiwe mkono wake, tena, naye akamwomba Mungu na mkono ukarudishwa tena, kama ulivyokuwa kwanza. Mfalme akajinyenyekeza na kumsihi mtu wa Mungu akae nyumbani kwake na kujiburudisha kabla hajaenda zake, naye atampa zawadi. Mtu wa Mungu akamwambia mfalme, "Ujaponipa nusu ya nyumba yako, sitaingia pamoja nawe, wala sitakula chakula, wala sitakunywa maji mahali hapa." Maana BWANA alimwagiza asile wala kunywa na wala asirudi kwa njia ile aliyoijia. Basi alienda kwa njia nyingine wala hakurudi kwa njia ile aliyoijia Betheli.

Basi nabii mmoja wa uongo, mzee, aliyekuwa akikaa Betheli, wanawe walimwendea wakamwambia kila kilichotokea kwa mfalme Yeroboamu siku ile pale Betheli. Maneno aliyosema mtu wa Mungu na majibu ya mfalme. Mzee yule, nabii wa uongo, akauliza, mtu huyu ameenda kwa njia gani? Wanawe walikuwa wameona alipopita na akatandika punda amfuate. Akaenda na kukuta mtu wa Mungu amekaa chini ya mti amepumzika. Akamwuliza kama ndiye mtu wa Mungu aliyetoka katika

Yuda, akasema ndiye; akamkaribisha kwake. Yule mtu wa Mungu akasema hawezi kwenda naye, wala kuingia naye kula au kunywa. Akamwambia BWANA amempa maagizo asile, asinywe huko na asirudi kwa njia aliyoijia. Yule nabii mwongo akasema, mimi nami ni nabii kama wewe, na malaika ameniambia kwa Neno la BWANA akisema, nikurudishe pamoja nami nyumbani kwangu ule chakula, na kunywa maji. Hata leo kuna manabii wa uongo kama huyu wanaoangamiza watu, hebu tujihadhari nao. Pale ambapo Mungu ametuambia mapenzi yake wazi kabisa, tusisikilize manabii wa uongo ambao siku hizi za mwisho wa historia ya dunia wapo wengi sana. Basi yule mtu wa Mungu akarudi na nabii wa uongo, kula na kunywa nyumbani mwake. Wakiwa mezani wanakula, Neno la BWANA likamjia yule nabii wa uongo, akamlilia yule mtu wa Mungu aliyetoka Yuda na kusema, "Bwana asema hivi, kwa sababu umeiasi kauli ya Bwana … bali umerudi, ukala chakula ukanywa maji, hapo alipokuambia, usile chakula, wala usinywe maji; maiti yako haitaingia kaburi la baba zako." Maskini, nabii wa uongo akawa tena ndiyo panga la kumkata.

Walipokwisha kula, nabii wa uongo akamtandikia punda kama zawadi ya mwisho, naye mtu wa Mungu akaenda. Alipokuwa njiani, alikutana na simba, aliyemwua. Maiti yake ikatupwa njiani, wala simba hakumla, basi huo ukawa ushahidi wa kutosikia maagizo ya BWANA. Simba alikuwa kati ya mzoga na punda. Watu waliopita wakaona mzoga unalindwa na simba, wakashangaa na kwenda kutoa habari katika mji wa nabii wa uongo. Nabii wa uongo aliyemrudisha mtu wa Mungu, alipopata habari akasema, "Ndiye yule mtu wa Mungu, aliyeiasi kauli ya BWANA; kwa hiyo BWANA amempambanisha na Simba, akamrarua, akamwua sawasawa na Neno la BWANA alilomwambia." Akawaita wanawe wamtandikie punda, akaenda akaitwaa maiti ya yule mtu wa Mungu na kuiweka juu ya punda, akamrudisha na kumzika kwenye kaburi lake mwenyewe, akafanya matanga na kumlilia wakisema "Aa! Ndugu yangu."
Hebu tujihadhari na marafiki wa uongo wanaotushauri kutenda kinyume na maagizo na Amri za BWANA. Nabii wa uongo akajifanya kwamba ni mpendwa sana wa nabii aliyekufa, na kuwaambia watoto wake, kwamba naye akifa azikwe na mtu wa Mungu. Neno alilolisema Mungu kuhusu madhabahu ya Betheli na madhabahu za uongo likatimia katika miji ya Samaria. Mtu wa Mungu asipotii maagizo ya Mungu anafungua mlango mkubwa wa kuingia hatarini. Bwana atusaidie kuwa waaminifu mpaka kufa.

*Tunahitaji neema, tunahitaji mwangaza kutoka kwa BWANA, ili kupitia Roho Mtakatifu tuweze kujua jinsi ya kuomba mambo hayo ambayo hakika tunayahitaji. Maombi yetu yakizingatiwa na Bwana yatajibiwa.

---

Kisa hiki kinakupatia fundisho gani? Mtu wa Mungu alimwambia maneno gani mfalme Yeroboamu? Kwa nini mkono wa mfalme ulikauka? Kwa nini simba alimwua yule mtu wa Mungu? Mtu wa Mungu anawezaje kuepuka hila za Shetani za uongo?

**SIKU YA 118**
**(Aprili 27)**

# Wafalme wa Yuda na Israeli

**- 1 Wafalme 14, 15 na 2 Mambo ya Nyakati 10**

Rehoboamu mfalme wa Yuda, alioa wake kadhaa kama, Binti Eliabu kaka wa Daudi, na wajukuu wa Daudi kama Maaka binti ya Absalomu. Alimpenda Maaka kupita wote na akafanya mpango wa kumrithisha ufalme Abiya, kijana wa Maaka. Daudi alishinda vita na kuteka nchi, na Sulemani alitawala, ila sasa Rehoboamu alikuwa na pungufu ya theluthi ya nchi ambayo Sulemani alitawala. Basi Mungu hakukusudia Israeli wawe taifa kubwa tu, bali watu wanaomcha Yeye. Rehoboamu alianza kutawala akiwa na miaka 41 na akatawala miaka 17 Yerusalemu, mama yake aliitwa Naama, Mwamoni. Naye pamoja na Yuda walifanya maovu na kumtia BWANA wivu kwa makosa yao. Walijenga mahali pa juu pa kuabudu miungu mingine, na maashera kwenye kila kilima kirefu, na chini ya kila mti wenye majani mabichi. Mwaka wa tano wa kumiliki Rehoboamu, Shishaki mfalme wa Misri alikuja na kuchukua hazina za nyumba ya Bwana na nyumba ya mfalme. Alichukua ngao za dhahabu, alizozifanya Sulemani, na mfalme akafanya ngao za shaba badala yake. Rehoboamu alipokufa, mwana wake Abiya alitawala badala yake; huyu Abiya ni tofauti na yule mtoto wa Yeroboamu aliyefariki.

Yeroboamu mfalme wa Israeli, hakuacha njia yake mbovu wala kukumbuka mkono wake uliokauka. Aliendelea kutumia makuhani bandia wa mahali pa juu. kwa watu wote, kila aliyetaka akamfanya wakfu, na makuhani wakatoa sadaka kwa miungu mahali pa juu. Jambo hili likawa dhambi machoni pa nyumba ya Yeroboamu, na usoni pa nchi. Siku hizo kijana wake aliyempenda, Abiya, akaugua. Naye akamtuma mkewe aende Shilo kwa nabii Ahiya, yule aliyemwambia atakuwa mfalme wakati akienda ukimbizi huko Misri. Alimwambia mkewe, atwae mikate kumi, keki na mtungi wa asali, na aulize kama hali ya kijana wangu itakuwaje? Mke wa Yeroboamu akaondoka kwenda Shilo kwa nabii Ahiya ambaye alikuwa kipofu kwa uzee, lakini BWANA alikuwa ameshamwambia kwamba mke wa Yeroboamu anakuja kuuliza mambo ya mwanawe, kwa maana anaumwa. Akaelezwa kwamba atajifanya ni mwanamke mwingine na si mke wa Yeroboamu, ila utakaposikia miguu yake ikiingia mlangoni mkaribishe, “karibu mkewe Yeroboamu, mbona unajifanya kuwa mwingine maana nimetumwa kwako wewe, mwenye maneno mazito. Nenda kamwambie Yeroboamu kwamba Mungu wa Israeli asema hivi, ‘Nilikutukuza miongoni mwa watu, nikakufanya uwe mkuu juu ya watu wangu Israeli. Nikamrarulia ufalme Daudi na kukupa wewe, walakini wewe hukuwa kama mtumishi wangu Daudi aliyezishika amri zangu na kunifuata kwa moyo wake wote asifanye ila yaliyo mema machoni pangu. Ila umekosa kuliko wote waliokutangulia na kujifanyia miungu mingine, na sanamu za kuyeyusha unikasirishe, na kunitupa nyuma. Tazama nitaleta mabaya juu ya nyumba ya Yeroboamu, na kumkata kila mwanamume. Nitawaondoa ukoo wake, kama vile mtu aondoavyo mavi, naye kila afaye mjini mbwa watamla, na afaye mashambani ndege wa angani watamla, kwa

kuwa BWANA amenena hilo. Akamwambia yule mke wa mfalme arudi nyumbani kwake, na atakapoingia mjini huyo kijana wake Abiya atakufa. Na Israeli wote watamlilia na kumzika, kwa maana ndiye peke yake wa Yeroboamu ambaye ataingia kaburini, kwa sababu limeonekana ndani yake jambo lililo jema kwa BWANA Mungu wa Israeli katika nyumba ya Yeroboamu. Akamwambia kwamba BWANA atajiinulia mfalme katika Israeli atakayeharibu nyumba ya Yeroboamu, kwa kuwa BWANA atawapiga Waisraeli kama manyasi yatikiswavyo majini, naye atawang'oa Israeli katika nchi hii njema aliyowaahidi baba zao; kwa vile wamejifanyia maashera ya miungu na kumkasirisha BWANA.

Basi mkewe Yeroboamu aliondoka, kwa huzuni ya mtoto wake na akijifikiria atamwambiaje mumewe mambo yale mazito. Mama huyu, alipofika tu kwenye kizingiti cha mlango wa nyumba yake, kijana wake Abiya akafa. Israeli wakamzika na kumwomboleza kama Neno la BWANA lilivyosema kupitia nabii Ahiya. Yeroboamu alitawala miaka 22 na akafariki; mwanawe Nadabu akarithi ufalme wake.

Mwaka wa 18 wa Yeroboamu kutawala, Abiya mwana wa Rehoboamu alianza kutawala juu ya Yuda. Mama yake alikuwa binti Absalomu, mwana wa Daudi. Akaziendea dhambi zote za babaye alizofanya, na moyo wake haukuwa mkamilifu kwa BWANA. Bali kwa ajili ya mema ya Daudi, Mungu alimwachia atawale. Bwana akasema Daudi alifanya yote niliyomwamuru, siku zote za maisha yake, isipokuwa kwa habari ya Uria, Mhiti. Basi kulikuwa na vita miaka yote kati ya Yeroboamu na Abiya, yaani, ufalme wa Yuda na Israeli. Abiya akafa na kuzikwa, na kijana wake Asa akatawala badala yake. Asa alianza kutawala mwaka wa 20 wa Yeroboamu mfalme wa Israeli, naye akatawala miaka 41, akafanya yaliyo mema kama babu yake Daudi, akafukuza mahanithi katika nchi na kuondoa sanamu zote alizozifanya baba yake. Akamwondoa hata Maaka, nyanya yake asiwe malkia kwa vile alikuwa amefanya sanamu za kuchukiza kwa Ashera, na akaikata sanamu yake na kuiteketeza penye kijito cha Kidroni. Siku moja Wakushi elfu elfu na magari 300 ya farasi walikuja kufanya vita na Asa, naye akamwomba Mungu amsaidie, akisisitiza kuwa 'Mungu hajali namba anaposaidia'. Mungu akamsaidia na wale Wakushi wakakimbia. Nabii Azaria alimjia Asa na kumwambia BWANA yupo pamoja naye, na akimtafuta, asimwache, ataonekana kwake, hivyo awe na ujasiri, maana kazi yake itakuwa na ijara. Asa akapata ujasiri na kutoa miungu ya kuchukiza ya nchi. Alikuwa mmoja wa wafalme wema wa Yuda. Alikuwa na makosa, ila moyo wake ulikuwa mkamilifu kwa BWANA siku zake zote. Ila hakuondoa mahali pa juu pa kutoa kafara kwa miungu, lakini moyo wake ulikuwa mkamilifu. Akaleta vitu alivyovitakasa BWANA kwenye madhabahu.

Kulikuwa na vita kati ya Asa na Baasha mfalme wa Israeli siku zao zote. Baasha akajenga Rama, ili asimwache yeyote kuingia kwa Asa mfalme wa Yuda. Ila Asa alifanya makosa ya kutoa fedha na dhahabu za hazina ya BWANA na kupeleka kwa mfalme wa Ben-Hadadi wa Shamu ili avunje mapatano yake na Baasha mfalme wa Israeli. Basi mfalme wa Shamu aliwapiga Waisraeli kwa sababu ya mkataba huo. Asa akaugua miguu akiwa mzee, naye akafa, na kuzikwa na babaze mjini mwa Daudi. Nadabu mwana wa Yeroboamu alianza kutawala juu ya Israeli mwaka wa pili wa Asa, mfalme wa Yuda. Akatawala miaka miwili tu kwa uovu na

kuiendea njia ya baba yake akiwakosesha Israeli.

Ushauri wa wazee kwa kawaida ni bora kuliko ule wa vijana, kwa sababu wazee wana uzoefu zaidi. Lakini ushauri bora zaidi ni ule ambao msingi wake umetokana na Neno la Mungu, kwa sababu Mungu hana kikomo katika hekima. Yeye amekuwepo milele. Ndiyo maana Yesu anasema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Mathayo 4:4 . Kuishi kwa Neno la Mungu ni njia ya uhakika ya kutofanya makosa maishani.

Mfalme Rehoboamu alikuwa na "vitabu" vitatu vikuu vya masomo kuhusu uongozi, yaani maisha ya Sauli, Daudi, na Sulemani. Inaonekana hakutumia muda mwingi kujifunza kutokana na makosa yao au mafanikio yao. Badala yake aliwasikiliza vijana wa rika lake. Alitangaza kwamba angetoza ushuru zaidi kwenye enzi yake, na kutembeza bakora. Angewanyanyasa watu, badala ya kuwa mtumishi wao. Yesu Mfalme, amekuita wewe na mimi kuwa viongozi tofauti leo "Yeyote anayetaka kuwa mkubwa kati yenu atakuwa mtumishi wenu" (Marko 10:43). Hata Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumikia watu, na kutoa nafsi Yake ili iwe fidia ya wengi.

*Dhambi Lazima Iwekwe Mbali ikiwa Maombi ya Uponyaji Yatajibiwa— Kwa wale wanaotamani maombi ya kurejeshewa afya, inapaswa kuwekwa wazi kuwa ukiukaji wa sheria ya MUNGU, ziwe za asili au za kiroho, ni dhambi, na ili wao waweze kupokea baraka Yake, lazima dhambi ikiriwe na kutupiliwa mbali.

---

Je, Asa alifanya vyema kutoa zawadi kwa Ben-Hadadi? Kwa nini Abiya mwana wa Yeroboamu alifariki? Familia ya Yeroboamu ilipewa adhabu gani? Dhambi ya Rehoboamu ilikuwa nini?

# Kings of Judah and Israel

| | |
|---|---|
| **Saul** | 1050-1010 BC |
| **David** | 1010-970 |
| **Solomon** | 970-930 |

## Judah (and Benjamin)

| King | Reign | | Character | Prophets |
|---|---|---|---|---|
| **1. Rehoboam** | 931-913 | 17 years | Bad | Shemaiah |
| **2. Abijah** | 913-911 | 3 years | Bad | |
| **3. Asa** | 911-870 | 41 years | Good | |
| **4. Jehoshaphat** | 870-848* | 25 years | Good | |
| **5. Jehoram** | 848-841* | 8 years | Bad | |
| **6. Ahaziah** | 841 | 1 years | Bad | |
| **7. Athaliah** | 841-835 | 6 years | Bad | |
| **8. Joash** | 835-796 | 40 years | Good | Joel |
| **9. Amaziah** | 796-767 | 29 years | Good | |
| **10. Uzziah (Azariah)** | 767-740* | 52 years | Good | Isaiah Micah |
| **11. Jotham** | 740-732* | 16 years | Good | |
| **12. Ahaz** | 732-716 | 16 years | Bad | |
| **13. Hezekiah** | 716-687 | 29 years | Good | |
| **14. Manasseh** | 687-642* | 55 years | Bad-repent | Nahum Habakkuk Zephaniah |
| **15. Amon** | 642-640 | 2 years | Bad | |
| **16. Josiah** | 640-608 | 31 years | Good | |
| **17. Jehoahaz** | 608 | 3 mo | Bad | |
| **18. Jehoiakim** | 608-597 | 11 years | Bad | Daniel Ezekiel Jeremiah |
| **19. Jehoiachin** | 597 | 3 mos | Bad | |
| **20. Zedekiah** | 597-586 | 11 years | Bad | |

Destruction of Jerusalem, 9th Av, 586 BC, Babylonian Captivity

## Israel (Ten Northern Tribes)

| King | Reign | | Character | Prophets |
|---|---|---|---|---|
| **1. Jeroboam I** | 931-910 | 22 years | Bad | Ahijah |
| **2. Nadab** | 910-909 | 2 years | Bad | |
| **3. Baasha** | 909-886 | 24 years | Bad | |
| **4. Elah** | 886-885 | 2 years | Bad | |
| **5. Zimri** | 885 | 7 days | Bad | |
| **6. Omri** | 885-874* | 12 years | Bad | Elijah Micaiah |
| **7. Ahab** | 874-853 | 22 years | Bad | |
| **8. Ahaziah** | 853-852 | 2 years | Bad | |
| **9. Joram** | 852-841 | 12 years | Bad | Elisha |
| **10. Jehu** | 841-814 | 28 years | Bad | |
| **11. Jehoahaz** | 814-798 | 17 years | Bad | Jonah Amos Hosea |
| **12. Jehoash** | 798-782 | 16 years | Bad | |
| **13. Jeroboam II** | 782-753* | 41 years | Bad | |
| **14. Zechariah** | 753-752 | 6 mo | Bad | |
| 15. Shallum | 752 | 1 mo | Bad | |
| **16. Menahem** | 752-742 | 10 years | Bad | |
| **17. Pekahiah** | 742-740 | 2 years | Bad | |
| **18. Pekah** | 740-732* | 20 years | Bad | |
| **19. Hoshea** | 732-712 | 9 years | Bad | |

722 BC Fall of Isreal / Assyrian Captivity

**SIKU YA 119**
**(Aprili 28)**

# Wafalme na Nabii Eliya-Mtishbi

**- 1 Wafalme 15-17 na 2 Mambo ya Nyakati 16**

Baasha wa Ahiya wa mbari ya Isakari akamfanyia fitina Nadabu na kumwua, akatawala mahali pake, na kuwapiga wana wote wa Yeroboamu wala hakumwacha hata mzao mmoja wa Yeroboamu sawasawa na Neno la BWANA, alilolinena kwa mtumishi wake Ahiya. Yeroboamu alikuwa amefanya makosa na kukosesha taifa zima la Israeli. Basi Nadabu alipokufa, Baasha alitawala na kuendelea kuwa na vita na Asa mfalme wa Yuda siku zao zote. Sasa wana ndugu walianza kupigana.

Baasha alitawala miaka 24, na kumfuata Yeroboamu kwa uovu na kuwakosesha Israeli. Ndipo Neno la BWANA lilimjia Yehu, juu ya Baasha akisema, "nilikuinua toka mavumbini na kukuweka uwe mkuu wa watu wangu Israeli, nawe umeiendea njia ya Yeroboamu, akasema atamtoa Baasha, na nyumba yake iwe kama nyumba ya Yeroboamu. Mtu wa kizazi cha Baasha anayekufa mjini, mbwa watamla, na afaye shambani, ndege wa angani watamla. Basi Baasha akalala na babaze, na Ela mwanawe akatawala katika Israeli, katika mwaka wa 26 wa mfalme Asa wa Yuda. Ela akatawala miaka miwili, naye alikuwa mlevi, na mtumishi wake Zimri, akaingia na kumpiga na kumwua. Zimri akaua wote wa nyumba ya Baasha, sawasawa na Neno la BWANA, kutoka kwa Yehu nabii. Zimri alitawala siku saba na kukatokea fujo katika Israeli, nao wakamweka Omri, jemedari, kuwa mfalme. Zimri alipoona vile, aliteketeza nyumba ya mfalme kwa moto, naye akaungua humo pia. Watu wakagawanyika kuwafuata watu wawili Tibni na jemedari Omri. Omri akamwondoa Tibni na akatawala mwaka wa 31 wa Asa kutawala katika Yuda, akajenga mji wa Samaria. Omri akafanya maovu kuliko waliomtangulia, kwa kuwakosesha Israeli kama Yeroboamu.

Omri alitawala kama miaka 7 hivi, akafa, na mwana wake Ahabu akatawala mahali pake. Ahabu alianza kutawala mwaka wa 38 wa Asa. Ahabu alitawala Israeli akiwa Samaria, mji aliouanza babaye, na akafanya maovu kuliko wote waliomtangulia, ikawa hata Yeroboamu alikuwa na nafuu kuliko yeye, kwani alimwoa Yezebeli binti wa Ethbaali mfalme wa Wasidoni, na akaenda kumtumikia Baali na kumsujudia. Ahabu akamghadhabisha BWANA kuliko wafalme wote waliotangulia kwani alifanya maashera. Yezebeli ni nembo ya mwanamke mwovu, na machukizo kwa Mungu kwa ajili ya ukahaba au kuabudu miungu mingine, hata leo, soma Ufunuo 2.

Baada ya mfalme Sulemani kufa, alizaliwa nabii aliyeitwa Eliya, mashariki ya mto Yordani. Bila shaka wazazi walimweka wakfu kufanya kazi ya Mungu. Alisikia mengi kuhusu wafalme wa Israeli na uovu wao akiwa mdogo. Eliya alikua wakati watu walikuwa wanachagua kati ya Mungu wa mbinguni au mabaali. Maana

ya jina lake lilikuwa - Mungu wangu ni Yehova. Kristo alimtaja Eliya kwa imani kuu aliyokuwa nayo japo alikuwa binadamu kama sisi; na hata Yohana mbatizaji kazi yake inafananishwa na Eliya. Basi, wakati ulipofika nabii huyu wa Mungu aitwaye Eliya, Mtishbi, alimwendea mfalme Ahabu kwa ujasiri, bila woga na kumwambia, "Kama BWANA, Mungu wa Israeli aishivyo, … hakutakuwa na umande wala mvua miaka hii, ila kwa neno langu." Watu wengi waliomba kwa Baali, Ashtorethi na Moleki, miungu ya sanamu isiyo na uwezo wowote.

Kisha BWANA akamwambia Eliya aende akajifiche katika kijito cha Kerithi, kinachokabili Yordani, na anywe maji hayo na kunguru ambao Mungu aliwaamuru wangemlisha huko. Yaani, Eliya alipoamka asubuhi, kwa kifungua kinywa, aliona kunguru wanamletea chakula. Viumbe vingine vya Mungu vinamtii, je, sisi binadamu? Basi aliend Kerithi, na Mungu akatimiza ahadi yake, ikawa baada ya siku kupita, kile kijito kilikauka kwa vile mvua ilikoma.

Neno la BWANA likamjia Eliya na kumwambia aende Sarepta na amemwagiza mwanamke mjane huko amlishe. Kristo alisema kulikuwa na wajane wengi katika Israeli ambao Eliya angeenda kwao, lakini aliend Sarepta kwa ajili huyu mama aliyekuwa mcha Mungu, mwenye imani. Akamkuta huyu mama mjane anaokota kuni. Basi akamwomba maji ya kunywa, alipoenda kuleta maji akamwomba ampe na kipande cha mkate, naye akasema "Kama BWANA, Mungu wako aishivyo, sina mkate, ila konzi ya unga katika pipa na mafuta kidogo katika chupa; nami naokota kuni mbili ili niingie nijipikie nafasi yangu na mwanangu, tuule tukafe." Eliya akamwambia asiogope, nenda kanifanyizie mkate kidogo mimi kwanza. Akamwambia ndipo ajifanyie wake na mwanawe. Pengine mama huyu alishangaa, kwamba huyu mtu ana ubinafsi wa kujifikiria yeye kwanza. Na ni kweli wapo watu ambao wanadai kufanya kazi ya Mungu leo, lakini wanaonekana kuwa watu wanaojali matumbo yao kuliko watu wanaowahudumia. Eliya hakuwa mtu wa namna hiyo, Hasha. Mjane huyu, alifuata maagizo, inawezekana hata mtoto aliuliza aliposikia harufu ya mkate. Mama akasema ni wa mgeni. Lakini hii ikawa ni baraka kwake, kwani imani na ukarimu wake ulizaa matunda makubwa. Eliya alimhakikishia kuwa, "Kama BWANA aishivyo, Mungu wa Israeli, lile pipa la unga halitapungua wala chupa ya mafuta haitaisha, hata siku ile BWANA atakapoleta mvua juu ya nchi." Basi alipotii kufanya yale aliyoagizwa, wakala siku nyingi, na ule unga kwenye pipa haukupungua, wala ile chupa ya mafuta haikwisha sawasawa na Neno la BWANA kupitia kwa mtumishi wake Eliya. Utii kwa Mungu una matunda mema siku zote, hata yakichelewa, jua tu kwamba yako njiani.

Mambo yote yaliyotangulia kuandikwa ni kwaajili ya kutufundisha sisi, ili kwa saburi na faraja tupate kuwa na matumaini. Mungu Yule Yule aliyemtayarisha Eliya riziki yake, atawaandalia watoto Wake leo hata hali ya ulimwengu iwe mbaya kwa kiasi gani. Hivyo, kanuni ya usalama wa chakula cha watoto wa Mungu ni hii: fanya kazi kwa bidii, kwa maana "Ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi asile" (2 Wathesalonike 3:10), kisha umwamini na kumtii Mungu. Kanuni hii haiwezi kushindwa kamwe, kwa kuwa Mwandishi wa -Zaburi asema, "Nalikuwa kijana na sasa ni mzee; Lakini sijamwona mwenye haki ameachwa, Wala wazao wake wakiomba chakula." Zaburi 37:25.

*"Maandiko yanatuambia," Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa." Yakobo 5:16. Kwa yule anayefanya maombi, hebu mawazo kama haya yawasilishwe: 'Hatuwezi kusoma moyo wako, au kujua siri za maisha yako. Hizo zinajulikana kwako mwenyewe tu na kwa MUNGU. Ukizikiri dhambi zako, ni wajibu wako kuziungama.

*udhani-dhania au ujasiri wa kujidanganya (presumption) hukaa jirani na Imani katika Kuombea Wagonjwa — Nimeona mambo mengi sana, katika kuwaombea wagonjwa yanayochukuliwa kwa kupitiliza (ushabiki), hadi nikahisi kwamba sehemu hii ya uzoefu wetu inahitaji mawazo thabiti, yaliyotakaswa, tusije kufanya ushabiki fulani kwa kudhania kwamba ni imani, na hata tukaiita ni imani, kumbe si chochote zaidi ya dhana. Watu waliochoka na shida ya ugonjwa wanahitaji kushauriwa kwa busara, ili wasonge kwa busara na hivyo kutoharibu mambo au kujiabisha; na wakati wanajiweka mbele za MUNGU kuombewa ili waponywe, hawapaswi kuchukua msimamo kwamba njia za urejeshaji wa afya kulingana na sheria za asili zinapaswa kupuuzwa. (tiba mbadala zinazofanya kazi, sisi tunapaswa kuwa na busara kuzitumia, ila kwenda hospitali na kuchunguzwa, kuchukua vipimo, maabara au xray ni muhimu kwenye dharura au hali tete, ila tunapaswa kujua jinsi ya kuzitumia tiba rahisi 8 Mungu alizotoa).


---

Umejifunza somo gani katika siku ya leo? Dhambi ya Baasha ilikuwa nini? Yezebeli alikuwa na tabia gani? Eliya alilishwa na nani kwenye kijito cha Kerithi? Mjane wa Sarepta aliagizwa nini na Eliya? Je, wewe leo ungepewa hayo maagizo ungefanyaje?

**SIKU YA 120**
**(Aprili 29)**

# Mwana wa Mjane wa Sarepta Afufuliwa

**- 1 Wafalme 17**



Basi mwana wa yule mjane wa Sarepta akaugua, na ugonjwa ukazidi hata akafariki. Akamfuata Eliya kwa uchungu na kusema, "Nina nini nawe, Ee Mtu wa Mungu? Je, umenijia ili dhambi yangu ikumbukwe, ukamwue mwanangu." Wengi hata siku hizi hufikiri wamepatwa na mabaya au maafa, kwa ajili ya uovu wao. Ni kweli kuwa mara zingine hili linaweza kutokea, ila si mara zote. Maana hata Ayubu alipatwa na maafa, ila hayakusababishwa na dhambi alizofanya. Ni vyema kumwomba Mungu na kujipeleleza kama Zaburi 139 inavyosema, "Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, unijaribu, uyajue mawazo yangu; uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, ukaniongoze katika njia ya milele." Basi Eliya alimwambia mjane, ampe yule mwanae, naye akamtwaa katika kifua chake na kumchukua chumbani mle alimokaa mwenyewe na kumlaza kitandani pake. Akamwomba Mungu akisema, "Ee BWANA Mungu wangu, Je! Umemtenda mabaya mjane huyu ninayekaa kwake hata kumfisha mwanawe. Akajinyosha juu ya mtoto mara tatu, akamwomba BWANA … nakusihi, roho ya mtoto imrudie ndani yake

tena. BWANA akaisikia sauti ya Eliya; na roho ya mtoto ikamrudia, akafufuka." Eliya akamtwaa mtoto toka orofani mpaka chini ya nyumba ile, akampa mama yake, akisema "tazama mwanao yu hai." Mungu alikuwa anamfundisha pia nabii wake kumtegemea na kumtumaini Yeye. Mjane hakuwa Mwisraeli bali alimtegemea Mungu. Mjane huyu alifurahi akasema, "Sasa najua ya kuwa wewe ndiwe mtu wa Mungu, na ya kuwa Neno la BWANA kinywani mwako ni la kweli." Alikuwa amekaa na Eliya miaka mitatu ila alikuwa na mashaka, japo alipata mwujiza wa kulishwa miaka yote hiyo. Tumwombe Mungu atuongezee imani.

Mfalme alimtafuta Eliya kwa hasira asimpate. Badala ya kuungama na kutenda mema ili BWANA amsamehe na kuirudishia nchi neema, yeye alikuwa anamtafuta mtu badala ya kuchunguza dhambi zake aziungame. Hata leo tusiwachukie watu wanaotuonya makosa yetu, bali tuwe tayari kutubu na kuungama dhambi zetu.

Mwaka wa tatu Neno la BWANA likamjia Eliya aende akajionyeshe kwa Ahabu mfalme wa Israeli na kusema nitaleta mvua. Eliya akaenda kilometa 200 hivi akajioneshe kwa Ahabu, wakati njaa nzito ikiendelea katika Samaria. Ahabu akamwita Obadia aliyekuwa mcha Mungu na mtumishi wa mfalme. Obadia alikuwa amewaficha manabii wa Mungu 100 na kuwalisha, wakati Yezebeli mke wa Ahabu alipowaua manabii wa BWANA. Ahabu alimwambia Obadia apite katika nchi akitafuta chemchemi za maji ili wanyweshe farasi na nyumbu wao ili wasipate hasara. Wakagawana na Ahabu kila mtu azunguke sehemu tofauti, na kumbe alipokuwa njiani, Obadia akamwona Eliya na kumtambua, kisha akaanguka kifudifudi akisema, "Ndiwe Eliya, Bwana wangu?" Eliya alimjibu ndiyo, na kumwagiza aende kwa mfalme Ahabu bwana wake, na kumwambia, "Tazama Eliya yupo." Obadia aliogopa, na kusema amekosa nini hata Eliya amtie matatani mikononi mwa mfalme. Akasema Ahabu ametuma watu wamtafute Eliya kila taifa, na ufalme. Watu waliotumwa waliposema Eliya hayupo, "aliwaapisha" kama ni ukweli hawakumwona. Obadia akasema, sasa unasema nenda kamwimbie Ahabu kwamba upo, na nikienda na Roho wa BWANA akakuchukua, uende nisikokujua, naye Ahabu asikuone, ataniua. Obadia akaomba aonewe huruma akisema "mimi mtumishi wako, namcha BWANA tangu ujana wangu. Nimewatunza manabii 100 wa BWANA kwenye pango baada ya Yezebeli kuwaua manabii wa BWANA. Obadia akarudia tena ile hatari ya kuuawa na mfalme. Eliya akamhakikishia kwamba atajionyesha mbele ya mfalme. Obadia akaenda kumwambia Ahabu, naye Ahabu akaenda kumlaki Eliya. Mfalme mwovu, aliamini Eliya ana uwezo wa kufanya mvua isinyeshe, bali hakuwa tayari kutubu dhambi zake, na mkewe na kuweka mji wake sawa ili neema ije kwenye taifa lake.

Ahabu alipomwona Eliya aling'aka "Je! ni wewe ewe mtaabishaji wa Israeli?" Eliya alijibu, si yeye ataabishaye Israeli, bali ni yeye Ahabu na nyumba ya baba yake kwa kuwa wameziacha amri za BWANA, naye amefuata mabaali. Mara nyingine tukipata adhabu kwa uovu wetu, tunasema ni fulani ametuchongea au kupeleka habari. Eliya, alimwambia mfalme awakusanye watu wa Israeli katika mlima Karmeli, na wale manabii 450 wa Baali na wale manabii 400 wa Ashera wakusanyike, na wote walao chakula mezani pa Yezebeli, mke wake Ahabu. Ahabu hakuwa na uchaguzi, bali alipeleka ujumbe kwa Israeli yote, na kuwaita waje kwenye mlima Karmeli,

pamoja na wale wa Baali, njaa na ukame vilikuwa vikali kwa kila mtu, hata ubishi au kutotii kuliisha.

Ayubu alisema "Lakini mimi najua ya kuwa Mtetezi wangu Yu hai, Na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, ……… nitamwona Mungu" Mungu atafufua watu atakapokuja tena mara ya pili. Ufufuo ni jambo linaloleta tumaini kwetu tunapowaaga wapendwa wetu kwa kifo. Tutatawatambua wapendwa wetu waliofufuliwa kwani kila mtu atakuwa na upekee wake, na hivyo Hatutaweza kuchanganya watu kwani watakuwa watu halisi na wala si roho zinazoelea.

*Ikiwa watachukua msimamo kwamba katika kuombea uponyaji lazima wasitumie tiba rahisi zilizotolewa na MUNGU ili kupunguza maumivu na kuisaidia asili katika kazi yake, hebu isije ikaonekana kwamba ni kuikana imani, wanachukua msimamo usiofaa. Huku siko kuikana imani; Inaendana kabisa na mipango ya MUNGU. Hezekia alipokuwa mgonjwa, nabii wa MUNGU alimletea ujumbe kwamba lazima afe. Alimlilia Bwana, na Bwana akamsikia mtumishi Wake na kufanya muujiza kwa niaba yake, akampelekea ujumbe kwamba miaka kumi na mitano ingeongezwa kwenye maisha yake. Sasa hapa Mungu angetumia Neno moja tu, na kisha angetibiwa kwa kuguswa mara moja tu kwa kidole cha Bwana, lakini maagizo maalum yalitolewa kuchukua tini na kuiweka kwenye sehemu iliyoathiriwa, na Hezekia akarejeshewa afya, yaani uzima wake ukarudishwa. Katika kila jambo tunahitaji kuenanda na mstari wa mipango na majaliwa ya MUNGU.

---

Eliya alilishwaje penye kijito cha Kerithi? Mjane wa Sarepta alimsaidiaje Eliya? Mjane wa Sarepta alisemaje mtoto wake alipokufa? Obadia alifanya jambo gani jema? Ni nani aliyewataabisha Israeli?

**SIKU YA 121**
**(Aprili 30)**

# Manabii wa Baali na Ashera Mlimani Karmeli

**- 1 Wafalme 18**



Eliya akawakaribia watu wote na kusema, "Mtasitasita katikati ya mawazo mawili hata lini? BWANA akiwa Ndiye Mungu, mfuateni; bali ikiwa Baali ni mungu, haya! Mfuateni yeye. Wale watu hawakumjibu neno." Eliya akasema amesalia yeye peke yake ambaye hakumpigia goti Baali. Akawaambia manabii wale wote waliokusanyika kwa wito wa Ahabu na Eliya, walete ng'ombe wawili, na wale manabii wa Baali wamchukue ng'ombe mmoja na kumkata kisha wamweke kwenye kuni ila wasiweke moto chini, naye pia atamtengeneza ng'ombe mmoja kwa ajili ya BWNA, na wala hatatia moto chini yake. Akaagiza manabii wa Baali waombe kwa jina la mungu wao, naye Eliya akasema ataomba kwa Jina la BWANA; na Mungu Yule ajibuye kwa moto, na awe Ndiye Mungu. Basi kwa vile yeye alikuwa peke yake, maana watu wengine wa Mungu waliuawa au kujificha, aliwaambia wale manabii wa Baali kwa kuwa ni wengi waanze wao kutoa sadaka. Basi wale Manabii wa uongo wakamtwaa ng'ombe waliyepewa, wakamtengeneza, na wakaliita jina la Baali toka asubuhi mpaka jioni ili alete moto. Lakini hapakuwa na sauti, wala hakuna aliyejibu. Nao wakaruka-ruka juu ya madhabahu waliyoifanya. Ilipofika adhuhuri, Eliya akawafanyia dhihaka, "mwiteni kwa sauti kuu, maana mungu

huyo; labda anazungumza, au ana shughuli au anasafiri, au labda amelala, sharti aamshwe. Manabii wa Baali walipiga kelele wakijikatakata visu na vyembe kama ilivyo desturi yao. Ilipofika jioni wakaanza kutabiri, lakini hapakuwa na sauti wala aliyejibu, wala aliyeangalia.

Watu walichoka mambo ya mabaali, na ndipo Eliya alipowaambia watu wote wamkaribie, na waliposogea kwake, akaitengeneza madhabahu ya BWANA iliyovunjika. Akatwaa mawe 12 kwa hesabu za wana wa Yakobo, aliyeambiwa jina lake litakuwa kubwa. Akajenga madhabahu kwa jina la BWANA … kisha akafanya mfereji ukiizunguka madhabahu. Akazipanga kuni, na kumkata ng'ombe vipande na kuviweka juu ya kuni. Akawaambia watu wajaze mapipa manne ya maji na kuyamwaga juu ya sadaka ya kuteketezwa na kuni, ili isionekane moto umefichwa. Akawaambia wamwage maji mapipa mengine manane. Jumla yakawa mapipa 12. Maji yakaizunguka madhabahu na kujaza mfereji. Ikawa wakati wa kutoa dhabihu ya jioni, Eliya akakaribia na kuomba, "Ee BWANA, Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka, na wa Israeli, na ijulikane leo ya kuwa Wewe Ndiwe Mungu katika Israeli, na ya kuwa mimi ni mtumishi wako, na ya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa Neno Lako. Unisikie BWANA, unisikie ili watu hawa wajue ya kuwa wewe, BWANA, ndiwe Mungu, na ya kuwa wewe umewageuza moyo wakurudie." Hata kabla ya ombi kumalizika, moto wa BWANA ukashuka, ukaiteketeza sadaka ya kuteketezwa, kuni, mawe na hata ukayaramba yale maji pakawa pakavu. Watu wote walipoona walianguka kifudifudi na kusema BWANA Ndiye Mungu, BWANA Ndiye Mungu. Mwujiza huu ulikuwa ni neema ya BWANA kuwajulisha wazi ni nani wamchague. Eliya akawaambia watu wawakamate wale manabii wa uongo wa Baali, asiokoke hata mmoja, walipowakamata Eliya akawachukua mpaka penye kijito cha Kishoni na kuwaua.

Eliya akamwambia Ahabu ainuke ale na kunywa maana, "pana sauti ya mvua tele." Basi Ahabu akiwa amechoka na mambo yaliyofanyika siku ile, japokuwa alikuwa ni mtu dhaifu wa tabia akiongozwa na mkewe kufanya uovu, alimtii nabii na akala na kunywa. Naye Eliya alipanda kilima cha Karmeli tena, akapiga magoti na kusujudu kifudifudi kuomba mvua toka kwa BWANA. Akamwambia mtumishi wake aende kutazama upande wa bahari kuona kama kuna wingu linaonekana. Mtumishi aliendа na kusema hakuna kitu, na mara saba alirudia tena kutazama. Ikawa baada ya safari ya saba, tazama wingu limetoka baharini, nalo ni dogo kama kiganja cha mkono. Eliya alikuwa na imani, kwa wingu dogo alijua BWANA ametenda, pia anatukumbusha tusikate tamaa au kuchoka, tukiomba mara moja, tusiache. Eliya akamwambia mtumishi wake aende kwa Ahabu na kumwamuru atandike farasi wake na ashuke kwenda ili mvua kali isimkute njiani. Japo mfalme alikuwa mwovu, bado Eliya alimheshimu na kumshughulikia. Kutii viongozi ni bora, isipokuwa pale wanapotaka tusimtii Mungu, ndipo tutachagua kumtii Mungu kuliko wanadamu. Baada ya muda mfupi, mawingu meusi yalionekana, na upepo, ikanyesha mvua nyingi sana. Ahabu akapanda farasi na kwenda kwake Yezreeli, kilomita kama 30 hivi. Nguvu na mkono wa BWANA ulikuwa na mzee Eliya naye akampa ujasiri wa kupiga mbio mbele ya Ahabu, akielekea kwenye giza na tufani mpaka akaingia naye Yezreeli.

Watu walikuwa na ukame wa zaidi ya siku 1000. Mvua ilikuwa inanyesha sasa kwa vile BWANA amewabariki. Wengi walimkubali BWANA siku ile, lakini wengine kama Ahabu na Yezebeli waliendelea kusitasita na tabia dhaifu za kushughulikia uovu.

**USIOGOPE!**

Eliya ni shahidi aliye hai kwamba tunapomtumaini BWANA kikamilifu tunawekwa huru na hofu.

Hebu tumwombe Mungu tujazwe na Roho Mtakatifu ili tupate uhuru kutoka kwa hofu zetu zote. Je, tunayumbayumba kati ya maoni mawili? Je, tunampenda Mungu na dunia pia? Je, tunaenda kanisani na pia kwa ulimwengu kufanya ibada huko? Je, tumeokolewa kwa neema na matendo? Leo, Yesu anatuuliza tufanye uamuzi. Tumpe Yesu moyo wetu wote! tumwelekezee Macho yetu YEYE. Mungu anahitaji tufishe tamaa na ufisadi wetu. Je, Mungu bado anataka kujidhihirisha kwenye ulimwengu usioamini leo? Ndiyo. Kunaweza kuwa hakuna moto kutoka mbinguni, lakini tukijisalimisha Kwake kikamilifu, kazi ya ajabu itafanyika kupitia ushahidi mkubwa wa uwepo Wake. Ndiyo maana anawaamuru watoto Wake, "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni".

*Wakala wa kibinadamu unapaswa kuwa na imani na unapaswa kushirikiana na uwezo wa Bwana, mtu akitumia kila namna ya nyenzo, akichukua faida ya kila kitu ambacho kulingana na akili yake ni cha manufaa, akifanya kazi kwa kupatana na sheria za asili; basi kwa kufanya hivyo haikani wala hazuii imani.

---

Kwa nini Ahabu alikuwa mfalme mwovu? Eliya alimsaidiaje Ahabu? Kwa nini kafara ya manabii wa Baali haikuteketea? Baali alikuwa na manabii wangapi? Kwa nini Eliya alimwongoza Ahabu kwenye giza? Katika marafiki zako, je, kuna anayesita sita unayeweza kumsaidia?

**SIKU YA 122**
**(Mei 1)**

# Eliya Apungukiwa Ujasiri na Kukimbia

**- 1 Wafalme 19**



Ahabu alimsimulia mkewe Yezebeli mambo aliyofanya Eliya na jinsi alivyowaua manabii wote wa Baali kwa upanga. Mwanamke huyu mwovu na mkorofi, Yezebeli, akapeleka ujumbe wa kumtishia nabii Elisha akisema, "Miungu na wanifanyie hivyo na kuzidi, nisipokufanya roho yako kesho, panapo wakati huu, kama roho ya mmojawapo wa hao manabii wangu wa Baali." Eliya aliposikia vile, alipatwa na woga ghafla, na ujasiri ukamtoka, akasahau kwamba Mungu anaweza yote, na hata huyu Yezebeli, angeweza kuangamizwa kama wale wengine walivyoangamizwa. Hii ni moja ya shida yetu wanadamu, siku moja tuna imani kubwa na siku ya pili tunatetemeka. Basi Eliya aliondoka kwa kukimbia ili ahifadhi roho yake, akafika Beer- sheba, mji wa Yuda na kumwacha mtumishi wake pale, ila yeye akaendelea katika jangwa mwendo wa siku moja, akaenda kuketi chini ya mti wa mretemu. Kwa sababu ya uchovu na kukata tamaa, roho yake ilifadhaika, akaomba kuwa ni afadhali afe, akisema, "yatosha; sasa, Ee BWANA, uniondolee roho yangu kwa kuwa mimi si mwema kuliko baba zangu." Eliya alitembea zaidi ya kilometa 250, akachoka. Naye akajinyosha chini na kulala chini ya mti wa mretemu. Mara malaika akamgusa na kumwambia ainuke na kula. Alipoangalia akaona mkate umeokwa juu ya mkaa na gudulia la maji kichwani pake. Chakula sahili, ndicho Mungu hutoa! Na ndicho chenye afya! Basi akaamka, akala na kunywa, na kujinyosha tena, akalala. Furaha ilimpata moyoni, akijua kuwa BWANA "anajua nilipo, na yeye mwenyewe ananitayarishia chakula."

Malaika wa BWANA akamwendea tena mara ya pili na kumgusa. Akamwambia ainuke, ale maana safari hii ni kubwa mno kwake. Ndipo akainuka tena, akala na kunywa na akaenda kwa nguvu ya chakula hicho kwa siku 40 mchana na usiku, alikuwa amefunga kula chakula. Akafika mlima Horebu au Mlima wa Mungu Sinai, ambapo Musa alipewa Amri Kumi. Akaona pango akaingia na kulala, na tazama Neno la BWANA lilimjia kusema, "unafanya nini hapa Eliya?" Naye akajibu "Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya BWANA, Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga; nami nimesalia mimi peke yangu; nao wananitafuta roho yangu waiondoe." Eliya alikuwa na wivu mzuri, wa kutamani watu wote wampende na kumtumikia Mungu. Na si wivu wa kuona mwenzako ana vitu vizuri na kutaka uvichukue wewe.

BWANA akamwambia Eliya atoke na kusimama mlimani mbele za BWANA. BWANA akapita, upepo mwingi ukaipasua milima, ukaivunja vunja miamba, ila BWANA hakuwemo katika upepo ule. Baada ya upepo, tetemeko la nchi likaja, lakini BWANA hakuwamo katika lile tetemeko. Baada ya tetemeko aliona moto, bali BWANA hakuwamo katika moto ule. Baada ya moto, sauti ndogo, na tulivu. Eliya alijifunika uso wake katika mavazi yake, akatoka na kusimama mlangoni mwa pango, na tazama sauti ikamjia, "unafanya nini hapa?" Eliya akarudia kusema ameona wivu mwingi kwa ajili ya BWANA, Mungu wa majeshi, kwa vile Israeli wameacha maagano na kuzivunja madhabahu za BWANA na kuwaua manabii wake kwa upanga, nami nimesalia peke yangu nao wanitafuta roho yangu waiondoe.

BWANA akamwambia Eliya aende, arudi njia ya jangwa la Dameski na amtie Hazaeli mafuta awe mfalme wa Shamu, na Yehu mwana wa Nimshi amtie mafuta awe mfalme wa Israeli; na Elisha mwana wa Shafati amtie mafuta awe nabii mahali pake.

Akasema atakayeokoka kwa upanga wa Hazaeli, Yehu atamwua, na atakayeokoka na upanga wa Yehu, Elisha atamwua. Mungu akampa habari Eliya kwamba kuna watu 7000 ambao hawajapiga goti kwa Baali wala kumbusu. BWANA akamwagiza kazi ya kufanya kabla ya kutwaliwa mbinguni.
Mungu alimpa Eliya muda wa kupona na kuondoa uchovu kwa chakula, mazungumzo, kazi mpya, na urafiki. Ni wakati wa utulivu na Mungu ndio ulimponya Eliya kimwili, kihisia, kiakili, kijamii, na kiroho. Ee Baba, tusaidie tunapokabidhi yote Kwako! Watu wa Mungu hawatakuwa huru kutokana na mateso; lakini wakiteswa na kuhangaika, huku wakistahimili ufukara na kuteseka kwa kukosa chakula, hawataachwa waangamie. Mungu huyo aliyemtunza Eliya hatampita hata kijana Wake mmoja aliyejitoa. Yeye ahesabuye nywele za vichwa vyetu anatujali, na wakati wa njaa tutashiba. Wakati waovu wanakufa kwa njaa na tauni, malaika watatulinda na kutupa mahitaji yetu. Kwake Yeye 'aendaye kwa haki' ana ahadi isemayo: Mkate atapewa; maji yake yatakuwa na uhakika na Maskini na wahitaji wanatafuta maji, wala hapana; ndimi zao zimekauka kwa kiu; Mimi, Bwana, nitawasikia, Mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha. Nitafunua vijito vya maji juu ya vilima, na

chemchemi katikati ya mabonde; nitageuza jangwa kuwa ziwa la maji, na mahali pakavu kuwa vijito vya maji.

*Katika Neno la MUNGU tuna maagizo yanayohusiana na maombi maalumu ya kuponya wagonjwa. Lakini utoaji wa ombi kama hilo ni tendo la wakfu kabisa na halipaswi kuchukuliwa bila kuzingatiwa kwa uangalifu. Katika visa vingi vya kuomba uponyaji wa wagonjwa, ile inayoitwa imani si kitu kingine tofauti na dhana.

---

Yezebeli alimtumia Eliya ujumbe gani? Kwa nini Eliya alikimbia? Ni fundisho gani tunalopata kuhusu kupewa chakula kwa Eliya? Mungu alikuwa na watu wangapi ambao hawajapiga goti kwa Baali?



**SIKU YA 123**
**(Mei 2)**

# Eliya Amtia Mafuta Mrithi Wake

**- 1 Wafalme 20**



Basi Eliya akaondoka akamkuta Elisha, mwana wa Shafati akilima, mwenye jozi ya ngombe 12. Elisha alitoka familia ya watu wenye uwezo. Basi Eliya akamwita karibu naye na kutupa vazi lake juu yake. Naye Elisha akawaacha ngombe akamfuata Eliya mbio, akasema nipe ruhusa nakuomba, nimbusu baba na mama yangu, kisha nitakufuata. Eliya alijua huu ni wito wa kuishi maisha ya kujikana ya nabii, na kuwa hatarini kwa chuki ya Yezebeli, lakini alichagua kumtumikia Mungu. Eliya akamruhusu aende na arudi, akasema, "Ni nini niliyokutendea." Akarudi na kisha akamfuata, akatwaa ile jozi ya ngombe akawachinja, akatokosa nyama ya ngombe kwa ile miti, akawapa watu, wakala. Alifanya hili ili asitazame nyuma na kuwa na kigeugeu, katika kumtumikia Mungu. Basi Elisha akainuka, akamfuata Eliya, akamhudumia.

Basi Ben-hadadi, mfalme wa Shamu akakusanya jeshi lake lote; nao walikuwapo wafalme thelathini na wawili pamoja naye, na farasi na magari, akakwea na kuuhusuru Samaria, akaupiga kwa vita. Akatuma wajumbe kwa Ahabu, mfalme wa

Israeli, wa uchokozi na kusema, “Fedha zako, dhahabu, wake zako, watoto wako, na vyote ni vyangu mimi!” Mfalme mwovu na dhaifu, Ahabu, alipata hofu akaanza kutetemeka na kujibu, “Ni kama ulivyosema bwana wangu, mfalme, mimi ni wako na vyote nilivyo navyo.” Mtu aliyeshindwa kusimama kwa Mungu, yupo tayari kuanguka na kuuza watoto, wake, na vitu vyake vyote. Basi wajumbe wakaenda kwa Ben- hadadi na kurudi na kusema, Ben-hadadi amesema, “Fedha yako, dhahabu, wake na wanao utanitolea mimi.” Akamwambia kesho yake, atatuma watumwa wake, ili watazame tazame nyumba yake na za raia wake, na kila kitu kipendezacho machoni pao watakitia mikononi mwao na kukichukua. Ndipo mfalme wa Israeli akawaita wazee wote wa nchi na kuwaambia waangalie kwani Ben-hadadi anataka madhara, maana ametuma kwangu kutaka wake, watoto, fedha na dhahabu kwamba ni vyake, nami sikumkatalia. Wale wazee wote wakamwambia asisikie wala asikubali hayo maneno ya mfalme wa Shamu. Basi Ahabu akatuma ujumbe akisema, “mwambieni bwana wangu mfalme, kila uliyotuma kumtaka mtumwa wako nitafanya ila neno moja tu siwezi kufanya.” Hapo ndipo alipopata ujumbe wa Ben-hadadi akiapa, “miungu wanifanyie hivi na kuzidi, yakiwa mavumbi ya Samaria yatatosha makozi ya watu wote walio miguuni pangu.” Ahabu alipata ujasiri na akarudisha majibu kwa mfalme wa Shamu “avaaye asijifu kama avuaye.” Naye Mfalme wa Shamu aliposikia hili, akiwa anakunywa pombe na wafalme wengine, aliwaambia watumwa wake wajipange nao wakajipanga.

Basi nabii alienda kwa Ahabu na kumwambia kama ameona makutano haya ya watu wengi ya wanajeshi wa Shamu. Akamwambia BWANA atawatia leo mkononi mwako nawe utajua ya kuwa ndimi BWANA. Ahabu alishangaa ni nani anaweza kuwashinda hawa. Ahabu akauliza ni nani atapanga vita? Nabii akamwambia ni yeye. Basi akawaandika vijana na maliwali wa majimbo nao walifika 232, na wana wa Israeli wote walikuwa 7000 wakatoka wakati Ben-hadadi akinywa pombe hata kulewa hemani mwake. Alikuwa na wale wafalme 32 waliomsaidia, walipofika aliambiwa wako watu kutoka Samaria, akasema wakamatwe hai. Vijana hawa wakapiga watu na Washami wakakimbia, na Israeli ikawafuatilia. Ben-hadadi mfalme wa Shamu akaokoka amepanda farasi na mfalme wa Israeli akatoka na kupiga Washami kwa pigo kubwa. Mtu wa Mungu akamwambia Ahabu akusanye nguvu kwani mwaka unaofuata, mfalme wa Shamu atakuja tena. Mfalme wa Shamu akasema, Waisraeli Mungu wao ni wa milima ndiyo maana wametushinda, lakini wakipigana kwenye tambarare watashindwa. Mwaka uliofuata, Ben-hadadi akaja tena apigane. Basi japo walikuwa kwenye tambarare, BWANA aliwashindia tena Waisraeli, na waliosalia wakakimbia. Ben-hadadi akakimbia kwao, na watumwa wake wakamwambia wafalme wa Israeli ni wenye huruma, hivyo wavae magunia na kamba vichwani na kumjia mfalme na kumsihi. Ben-hadadi akafanya hivi, akiwa amevaa gunia akaenda kwa Ahabu na kusema, “mtumwa wako Ben-hadadi asema, “roho yangu, nakusihi iishi.” Ahabu akauliza kama Ben-hadadi yu hai, nao walisema ndiyo. Kisha mfalme wa Shamu alikuja na kusema atarudisha miji aliyomnyang’anya baba yake Ahabu. Ahabu akamwacha kwa mapatano hayo. Ahabu akapata kiburi kwamba mfalme mkuu kama Ben-hadadi anampigia magoti, hivyo akamwacha, na kumpa ufalme wake, jambo lisilokuwa la hekima. Mungu akamwonesha kosa la Ahabu, kwa kitendawili kinachofuatia.

Basi mwana mmoja wa manabii akamwambia mwenzake ampige, na mwenzake akakataa. Ndipo simba alimwua yule aliyekataa kumpiga mwingine. Kisha huyu mwana wa nabii aliona mwingine anapita na kumwomba ampige, naye akampiga na kumtia jeraha. Kisha yule nabii aliye na jeraha aliendakungoja njiani mwa mfalme, akiwa amejibadilisha kwa kilemba juu ya macho yake. Akamwambia mfalme fumbo, "Mtumwa wako aliingia katika pigano, na tazama mtu mmoja akanigeukia, akaniletea mtu, akaniambia, Umlinde mtu huyu; akipotea kwa njia yoyote, roho yako itakuwa mahali pa roho yake, au utatoa talanta ya fedha. Ikawa mtumishi wako alipokuwa akitenda haya na haya, yule akaenda zake. Mfalme wa Israeli akamwambia, Ndivyo itakavyokuwa hukumu yako; umejihukumu mwenyewe." Yule mwana wa nabii akatoa kilemba haraka kumwonesha mfalme jeraha. Akamwambia, BWANA asema hivi, kwa sababu umemwachilia ….. mtu niliyemweka mikononi mwako ili aangamizwe kabisa, roho yako itakuwa mahali pa roho yake, na watu wako mahali pa watu wake." Ahabu, mfalme wa Israeli akaenda nyumbani kwake na moyo mzito, mwenye hasira, akaja Samaria.

Unaweza kufikiri kwamba mafanikio ya kazi ya Mungu katika jumuiya yako yanategemea mtu anayejulikana zaidi kuliko wewe—labda mchungaji, mwinjilisti, au mzee wa kanisa. Lakini vipi ikiwa wewe ni msichana au mvulana wa Mungu ambaye anakuita kufanya kile ambacho hawawezi kufanya? Vipi ikiwa wewe ni mwana au binti wa Mungu ambaye mtu atakusikiliza wakati ameacha kumsikiliza kila mtu? Pengine mama, baba, kaka, dada, binamu, mjomba, au bibi wametanga mbali, nawe waweza kuwafikia, fanya hivyo basi. Mambo makubwa yanaweza kutokea wakati akina Eliya kati yetu wanaposimama kwa ujasiri na kufanya tofauti. Mambo makubwa zaidi yatatokea wakati sisi sote tutafanya sehemu yetu wakati Mungu anapotuita. Hata mambo yawe mabaya kiasi gani, tusisahau kwamba Mungu ameahidi, akisema: "Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha."—Waebrania 13:5.

*Watu wengi hujiletea magonjwa kwa kujifurahisha au kujiendekeza kwao wenyewe. Hawajaishi kulingana na sheria ya asili au kanuni za usafi wa moyo thabiti. Wengine wamepuuza sheria za afya katika tabia zao za kula na kunywa, kuvaa, au kufanya kazi. Mara nyingi aina fulani ya uovu ndiyo sababu ya udhaifu wa akili au mwili. Ikiwa watu hawa wangepata baraka ya afya, wengi wao wangeendelea kufuata njia ile ile ya uasi wa kutozingatia sheria za asili na za kiroho za MUNGU, wakifikiri kwamba ikiwa MUNGU atawaponya katika kujibu maombi yao, basi wao wako huru kuendelea na mazoea yao mabaya na yasiyofaa na kuendeleza kujifurahisha na tamaa za mwili potovu bila kujizuia Ikiwa MUNGU angefanya muujiza kuwarudishia watu hawa afya, angekuwa akiwatia moyo kuitenda dhambi.

---

Umepata fundisho gani kwenye kisa hiki? Kwa nini Elisha alipasua kuni na kuchinja ng'ombe? Ahabu alishindaje vita na Shamu? Kwa nini BWANA alisema ni kosa kumwacha mfalme wa Shamu? Ungekuwa wewe na unajua uovu wa Ahabu je, ungeendelea kuhusiana naye?

**SIKU YA 124**
**(Mei 3)**

# Shamba la Nabothi

**- 1 Wafalme 21**

Mfalme Ahabu aliyetawala Israeli yote, alikuwa tajiri bali mwenye kijicho na wivu mno. Alikuwa na ikulu mbili, Samaria na Yezreeli. Siku moja akitazama nje ya dirisha lake kwenye nyumba yake ya kifalme. Aliona shamba la mizabibu la Nabothi, Myezreeli. Ahabu akamwambia ampatie shamba lake mfalme ili apande mboga, maana ni karibu na nyumba yake naye atampa shamba lingine zuri zaidi au fedha. Nabothi akamwambia Ahabu kwamba shamba hili ni urithi toka kwa baba zake. Ahabu akaenda kwake na moyo mzito na tena amekasirika, kwa sababu Nabothi amemwambia hawezi kumpa shamba lake. Akajilaza kitandani kama mtoto mdogo anayedeka na kugeuza uso wake akazira kula. Watu wengine siku hizi wana tabia ya kutaka kila kitu kiende wanavyotaka, hata kama ni jambo baya. Kama hataki kuambiwa jambo anachukia na kuzira. Hili ni jambo baya.

Mke wake Ahabu, yule mama aliyejulikana kwa uovu, na kuabudu sanamu alikuja na kumkuta amesononeka, mwenye huzuni na amezira chakula. Akamwuliza sababu yake, naye akamweleza. Yezebeli akacheka kicheko cha kejeli na kumwambia, wewe ndiyo mfalme, na wala si Nabothi, nenda ondoka ule chakula, moyo wako ufurahi; mimi nitakupa shamba la mizabibu la Nabothi. Basi mwanamke huyu kwa uovu



akaandika barua kwa jina la Ahabu na kuzitia muhuri wake, akazipeleka kwa wazee na kwa watu wenye nguvu wa mji wake waliokaa pamoja na Nabothi. Akaandika kwenye zile barua, "pigeni mbiu ya watu kufunga, mkamweke Nabothi juu mbele ya watu. Mkainue watu wawili, watu wasiofaa, ili wamshitaki na kumshuhudia uongo kwa kunena, umemtukana Mungu na mfalme. Kisha mchukueni nje, mkampige kwa mawe, ili afe." Basi wazee waovu wa mji, wakimfuata kiongozi wao Yezebeli na Ahabu wakafanya vile walivyoagizwa katika zile barua. Wakapiga mbiu na kufunga na kumshuhudia Nabothi uongo kuwa amemtukana Mungu na mfalme. Wakamchukua Nabothi na kumpiga mawe hata akafa, kisha wakampelekea Yezebeli taarifa ya kutimiza kazi hiyo. "Nabothi amepigwa kwa mawe na amekufa." Yezebeli aliposikia, akamwambia Ahabu ainuke na kumiliki lile shamba Nabothi alilokataa kumpa, maana hayuko hai, kwani amekufa. Basi Ahabu akatoka amiliki shamba bila aibu au masikitiko.

Ndipo Neno la Mungu lilipomjia Eliya nabii aondoke na kukutana na Ahabu huko Samaria shambani kwa Nabothi siku aliyokwenda ili amiliki shamba, na kumwambia, "BWANA asema hivi, je! umeua, ukatamalaki?" Eliya akamwambia BWANA asema hivi "Mahali pale mbwa walipoiramba damu ya Nabothi, mbwa watairamba na damu yako." Ahabu akashangaa Eliya amejuaje haya na kusema "Je, umenipata ewe adui yangu? Akamwambia, nimekupata kwa sababu umejiuza utende yaliyo mabaya machoni mwa BWANA." Eliya akamwambia Mungu atamwangamiza na kumkata kila mwana wa kiume wa uzazi wake, kama alivyofanya nyumba ya Yeroboamu, na Baasha. Kwa ajili ya machukizo yao na kumghadhibisha na kuwakosesha Israeli. Tena mbwa watamla Yezebeli katika kiwanja cha Yezreeli, na mtu wa nyumba ya Ahabu afaye mjini, mbwa watamla, na yeye afaye mashambani ndege wa angani watamla. Ahabu alitenda uovu kupita wote, na mkewe alimchochea.

Ahabu aliposikia haya alirarua mavazi yake akavaa magunia kwa kujutia na kwenda kwa upole. Basi Mungu akaghairi yale mabaya yasitokee wakati wake ila kwa siku za wanawe. Yote ni shida tu, kwa ajili ya uovu, yaani, wanawe wakafuata wanayoona na kuwa kama mama na baba.
Uovu wake ukafuata siku za mtoto wake, ni jambo la kusikitisha. Mungu haachi uovu usipate adhabu, bali mara zingine inachukua muda, ila uovu una mshahara wake mwishowe.

Baadhi ya viongozi wamechukua mali walizopenda kwa nguvu toka mikononi mwa watu wengine na kupoteza haki za wanyonge wakifikiri Mungu hatafanya kitu. Mungu ana rehema na uvumilivu. Ahabu na mkewe walipewa nafasi nyingi za kuungama na kujirudi, lakini walizama katika uovu zaidi na kujisahau. Alipoendewa na nabii shambani, angelirudisha shamba hili kwa watoto wa Nabothi na kuungama. Mwombe Mungu akusaidie usifuate njia ya Ahabu.

Ushirikiano wa Ahabu na Yezebeli ulikuwa wa kushirikiana uovu. Walikuwa sumu ya ibada ya Kweli. Mambo aliyofanya kumfurahisha mume wake yalikuwa mabaya, na katika kisa cha Nabothi, yalikuwa ya udanganyifu,uchokozi na uuaji. Zawadi ya Mungu ya ndoa, iliyokusudiwa kuwatia moyo waume na wake kuhudumiana na kuhudumia wale walio karibu nao, iligeuzwa kuwa njia ya kutia moyo ubinafsi

na uchoyo wa kila mmoja wao. Ikiwa bado unatafuta mwenzi, usitafute au kutulia kwa mtu ambaye huleta mabaya zaidi ndani yako. Nawe usiwe mtu wa kuleta mabaya kwenye moyo wa mwenzi wako. Omba Mungu akusaidie kuwa mke/mume unayepaswa kuwa, ili ndoa yako ibariki mwenzi wako na iwe chanzo cha msaada kuliko maumivu kwa watu wanaokuzunguka.

*Ni kazi iliyopotea kuwafundisha watu kumtazama MUNGU kama mponyaji wa udhaifu wao, pasipo kuwafundisha pia kuacha mazoea yasiyofaa, yale ambayo yanapingana na afya. Ili kupokea baraka Yake katika kujibu maombi, lazima waache kufanya uovu na kujifunza kutenda vyema. Mazingira yao lazima yawe safi, mwenendo wao wa maisha uwe sahihi. Lazima waishi kwa kupatana na sheria ya MUNGU, asili na kiroho.

---

Ahabu alitaka nini toka kwa Nabothi? Mfalme alifanya nini baada ya kukataliwa shamba? Mke wake alitoa ushauri gani? Eliya alileta ujumbe gani toka kwa Mungu? Kwa nini Mungu alisema mabaya yatatokea siku za mtoto wake?

**SIKU YA 125**
**(Mei 4)**

# Siku za Mwisho za Ahabu

**- 1 Wafalme 22 na 2 Mambo ya Nyakati 18**

Kukawa na miaka mitatu ya amani, kisha mfalme wa Yuda, Yehoshafati akamwendea Ahabu, mfalme wa Israeli. Ahabu akasema mji wa Ramoth–Gileadi ni wao na wauchukue kutoka kwa Washami. Basi akazungumza na mfalme Yehoshafati kwamba waende pamoja vitani ili kuchukua mji huu. Yehoshafati akasema "Mimi ni kama wewe, na watu wangu ni kama watu wako, na farasi zangu ni kama farasi zako." Mfalme Yehoshafati alimcha Mungu, lakini akajiingiza kufanya urafiki na Ahabu, aliyekuwa adui wa Mungu. Ahabu akakusanya manabii 400 wa uongo na kuwauliza kama aende kuutwaa Ramoth-Gileadi, nao wakasema, "Kwea kwa kuwa BWANA atautia mkononi mwa mfalme." Yehoshafati akaona mashaka na manabii hawa wa uongo na akamwuliza Ahabu, "Je! Hayupo hapa nabii wa BWANA tena, ili tumwulize yeye? Ahabu akasema yupo mtu mmoja anaitwa Mikaya, ila namchukia, kwa sababu hanibashirii mema, ila mabaya. Yehoshafati akasema, La! mfalme asiseme hivyo. Basi Ahabu akamwambia mjumbe amwite Mikaya, na Ahabu na Yehoshafati walikuwa wakikaa kila mtu katika kiti chake cha enzi, na mavazi ya kifalme langoni mwa Samaria huku manabii wa uongo wakifanya unabii mbele yao. Zedekia nabii wa uongo akajifanyia pembe na kusema, "utawasukuma Washami, hata waharibike." Na wote wakasema, kwea ufanikiwe.

Basi walipokuwa wakienda kwa mfalme, yule mjumbe aliyekwenda kumleta Mikaya akamsihi akisema, "Nakusihi useme maneno mema kwa mfalme." Ila Mikaya alisema atasema tu yale BWANA atakayomwambia. Wakaingia kwa wafalme na Ahabu akasema, Je! Mikaya, tuende Ramoth-Gileadi kupiga vita, au tunyamaze? Mikaya akajibu kwa kejeli "kwea ufanikiwe." Mfalme akastuka na kusema, "mara ngapi nikuapishe usiniambie neno ila yaliyo kweli, kwa Jina la BWANA?" Ndipo akasema kweli aliyoambiwa na BWANA, "Naliwaona Waisraeli wote wametawanyika milimani, kama kondoo wasio na mchungaji." BWANA akasema, Hawa hawana bwana; na warudi kila mtu nyumbani kwake kwa amani." Ahabu akamwambia Yehoshafati "Je! sikukuambia, hatanibashiria mema, ila mabaya? Mikaya akasema alimwona BWANA katika kiti Chake cha enzi, na jeshi lote la mbinguni, na sauti ilisikika ikisema, ni nani atamdanganya Ahabu kukwea Ramoth-Gileadi akaanguke? Basi huyu akasema hivi na yule hivi. Basi pepo mmoja akaja na kusema atamdanganya Ahabu kupitia vinywa vya manabii wake kwa uongo. Ahabu alipenda kumtumikia Shetani, na kisha kuwalaumu watumishi wa Mungu yalipotokea mabaya. Basi Mikaya akamwonya kwamba kuna pepo la uongo kwa manabii wake wote, Naye BWANA amenena mabaya juu yake. Zedekia nabii wa uongo akitaka kujipendekeza kwa mfalme, akasogea na kumpiga kofi Mikaya akisema, "Roho wa BWANA alitokaje kwangu ili aseme na wewe?" Mikaya akamwambia ataona siku atakapoingia chumba cha ndani ili ujifiche. Ahabu akasema wamchukue Mikaya wamweke gerezani, wamlishe chakula na maji ya shida, mpaka siku ile atakaporudi

kwa amani. Mikaya akasema, "ukirudi kwa amani, BWANA hakusema nami, sikieni watu wote." Basi wafalme Yehoshafati na Ahabu wakakwea kwenda Ramoth-Gileadi. Ahabu akiwa amevaa nguo za kiraia ila Yehoshafati nguo za kifalme. Mfalme wa Shamu aliwaambia askari wake wasisumbuke kupiga wanajeshi wa kawaida, bali mfalme wa Israeli peke yake. Basi wakuu wa jeshi la Shamu walimwona Yehoshafati na kumfuata wakifiri ni Ahabu, mfalme wa Israeli, naye Yehoshafati akapiga kelele, na wakuu hawa wakaona si yeye, wakageuka nyuma wasimfuate. Mtu wa haki Yehoshafati alijiingiza ubia na mtu mwovu, na hili ni fundisho tunapotaka kufanya mapatano, urafiki au biashara na watu wasiomjali Mungu na kuwatoa watoto wetu waoe au waolewe na watu wenye ujasiri katika kumkufuru Mungu wa mbinguni waziwazi. Hakika Mungu wetu ni mwenye rehema, mara nyingi tunajiingiza pabaya, Naye anafanya jitihada juu chini ili kutuokoa. Anatuma watumishi Watuonye, ila tunapenda kusikia mambo mazuri kuhusu sisi na si ya maonyo ili tubadilike. Wako washiriki wengi wanaowaambia viongozi wao "sema mambo mazuri ya kutusifu, ukitukaripia, hatutakulipa mshahara au vizawadi."

Kisha mtu mmoja alivuta upinde kwa kubahatisha na kumpiga Ahabu mahali pa kuungana mavazi yake, pasipokuwa na kinga yoyote ya chuma, naye akamwambia mwendesha gari lake, "geuza mkono wako unichukue toka uwanja wa vita, kwa kuwa nimejeruhiwa sana." Siku hizo ilikuwa lazima mfalme aende vitani, si kama leo. Pigano likazidi, mfalme akawa mahututi akaegemea gari lake, hata jioni akafa kwa kuvuja damu nyingi. Ikapigwa mbiu jeshini jua likichwa, kila mtu aende shambani kwake. Maiti ya mfalme ikachukuliwa Samaria. Wakaliosha gari lake kwenye kisima cha maji, walipooga makahaba, na mbwa wakaramba damu yake sawasawa na Neno la BWANA alilonena kupitia kwa nabii Eliya. Ahabu akalala na babaze na Ahazia mwanawe akatawala mahali pake.

Yezebeli yeye alikufa, walinzi wake walipomrusha nje ya dirisha ghorofani huko Yezreeli. Damu yake ikaenda ukutani na kwenye farasi. Walipokuja ili wamzike, walikuta mifupa ya fuvu la kichwa na miguu na mikono tu kwani mbwa walikuwa wamemla mwili wote kama vile nabii Eliya alivyotabiri. Mungu anasema anachokimaanisha, na anamaanisha anachosema, unabii na ahadi Zake, zinatimia mara zote. Mioyo ya wanandoa hawa ilikuwa na ufisadi wa kutisha, na wakaitikisa nchi nzima kwa ujeuri wao. Japo Yezebeli hakuwa mke wa kwanza, alikuwa analitawala taifa na yule mfalme wa Israeli, naye aliita watu wake 850+ wakalishwa na taifa la Mungu kila mlo, kila siku. Watu wa Mungu wakatoa sadaka ili kuwalisha watumishi hawa wa Adui Baali. Cha kuomba leo ni "Usinipite Mwokozi, unisikie, unapozuru wengine usinipite" maana tunamhitaji Bwana Awe mgeni wa mioyo yetu, ili tusifanye maamuzi yenye uovu unaofanya masikio yapate mwasho, kama yale ya kupata mwenzi wa maisha aliye na tabia chafu, mpaka anakuwa methali ya dunia nzima, maana leo tuna msemo "ameoa Yezebeli".


*Maombi ya Uponyaji wa Kimuujiza Yanaweza Kusababisha Ushabiki (au kupitiliza) - "Kwa nini," mmoja baada ya mwingine wanauliza, "maombi hayatolewi kwa ajili ya uponyaji wa miujiza wa wagonjwa, badala yake unatolewa kwa ajili ya vituo vingi vya afya vya Sanitarium vilivyoanzishwa?" Hili likifanyika, ushabiki mkubwa utazuka katika safu zetu. Wale wanaojiamini sana wangeanza utendaji.

Kwa nini Ahabu aliendα vitani? Aliendα nα nani? Kwa nini hakuvaa vazi la kifalme? Nabii wa uongo alimwambia nini Ahabu? Je, unapenda kusikia maneno matamu matamu ya uongo, au magumu ya kweli yatakayokusaidia? Kwa nini Ahabu alimfunga Mikaya? Ahabu alipatwa na nini vitani? Ni nani alikuwa nabii wa kweli?

**SIKU YA 126**
**(Mei 5)**

# Yehoshafati, Ahazia na Eliya

**- 1 Wafalme 22, 2 Wafalme 1 na 2 Mambo ya Nyakati 17-19**



Yehoshafati mwana wa Asa, alianza kutawala Yuda akiwa na miaka 35, katika mwaka wa nne wa utawala wa Ahabu huko Israeli. Akatawala miaka 25, akaenda katika njia njema za babaye Asa, wala hakugeuka. Babaye Asa alipata ujumbe kupitia nabii Hanani akisema, "kwa maana macho ya BWANA hukimbia-kimbia duniani mwote, ili ajionyeshe mwenye nguvu kwa ajili ya hao waliokamilika moyo kuelekea kwake." Ujumbe huu ni wetu sote leo, tusifikiri BWANA haoni, anajua kila kitu, tukijisalimisha kwake atajidhihirisha kwetu.

Lakini Asa hakupenda kuonywa, alimweka nabii gerezani, pia mahali pa juu pa kuabudia miungu migeni hakupabomoa. Mtoto wake Yehoshafati akafanya amani na mfalme wa Israeli. Naye aliwaondoa mahanithi, makahaba, na sanamu ambapo watu walifanya ibada za uovu. Yehoshafati akafanya merikebu kwenda Tarshishi kuchukuka dhahabu ya Ofiri ila merikebu zilivunjika huko Esion-geberi. Yehoshafati alipokufa, Yehoramu mwanawe akatawala badala yake.

Ahazia mwana wa Ahabu alitawala baada ya baba yake na akafanya yaliyo mabaya machoni pa BWANA kama babaye. Ahazia akaanguka katika dirisha la chumba chake ghorofani, huko Samaria na akaugua, kisha akatuma wajumbe waulize kwa Baal-zebubu mungu wa Ekroni kwamba atapona ugonjwa ule. Malaika wa BWANA akamwambia Eliya aondoke na kwenda kuonana na wale wajumbe wa mfalme na kuwauliza, "Je! ni kwa sababu hapana Mungu katika Israeli, hata mnakwenda kuuliza kwa Baal-zebubu, mungu wa Ekroni?" Wakapewa ujumbe kwamba mfalme Ahazia hatashuka katika kile kitanda alichokipanda, bali hakika atakufa, na Eliya akaondoka. Wajumbe wakarudi na mfalme akashangaa mbona wamerudi mapema hivyo. Nao wakajibu, Mtu alitokea… akatuambia turudi kwa mfalme aliyetutuma na kumwambia, "Je! ni kwa sababu hapana Mungu katika Israeli, hata mnakwenda kuuliza kwa Baal-zebubu, mungu wa Ekroni?" Basi kwa ajili ya hayo hutashuka katika kile kitanda ulichokipanda, bali hakika utakufa."

Mfalme akauliza mtu huyu alikuwa wa aina gani, nao wakamwambia alikuwa amevaa vazi la manyoya, tena amejifunga shuka ya ngozi kiunoni mwake. Naye akajua ni Eliya Mtishbi. Basi mfalme akatuma akida na askari 50 kwa Eliya, wakamkuta ameketi juu ya kilima na wakamwamrisha. "Ewe mtu wa Mungu mfalme asema shuka." Eliya akasema kama yeye ni mtu wa Mungu, moto ushuke toka mbinguni na uwateketeze. Basi moto ulishuka na kuwaangamiza. Akatuma tena akida na askari 50 nao wakapata shida ile ile. Mara ya tatu, mfalme akatuma tena akida na askari 50 wengine. Huyu akida alipanda juu ya kilima na kupiga magoti kwa Eliya akimsihi sana kwa kusema, "Ee Mtu wa Mungu, nakusihi, roho yangu, na roho za watumishi wako hawa hamsini ziwe na thamani machoni pako." Maana moto ulishuka ukateketeza 50 mara mbili, jumla mia moja. Akasisitiza "Laiti sasa roho yangu na iwe na thamani machoni pako." Mungu anapendezwa na unyenyekevu, kwani wale wengine waliona ni wenye nguvu za jeshi na wametumwa na mfalme, wakaanza kumwamrisha mtu wa Mungu badala ya kuwa na adabu. Malaika wa BWANA akamwambia Eliya ashuke na kwenda pamoja nao bila woga, kwa mfalme. Naye Eliya akarudia ujumbe wa kwa nini aende kwa mungu wa Ekroni? Na kwamba kwa sababu hiyo atakufa. Mfalme Ahazia akafa, kama Neno la Mungu lilivyokuja. Na Yoramu mwana wake akatawala mahali pake.

*Kuchukua Hatua Sahihi Sio Kuikana Imani Katika Maombi ya Uponyaji —Wengi wanaotafuta rehema ya uponyaji wa Bwana wanafikiri kwamba lazima wawe na jibu la moja kwa moja na la haraka kwa maombi yao au imani yao ina hitilafu. Kwa sababu hii, wale ambao wamedhoofishwa na magonjwa wanahitaji kushauriwa kwa busara, ili watende kwa hekima. Hawapaswi kupuuza wajibu wao kwa marafiki ambao wanaweza kuwasaidia kuishi, au kupuuza kutumia wakala wa asili (au tiba mbadala) kwaajili ya urejeshaji wa afya.

---

Eliya alikuwa anavaa mavazi gani? Wanajeshi 50 wa mwisho waliponaje walipoenda kwa Eliya? Kwa nini mfalme Ahazia alifariki? Macho ya BWANA yanaenda huko na huko kuangalia nini?

**SIKU YA 127**
**(Mei 6)**

# Nabii Eliya Atwaliwa Mbinguni - Ni Baraka Gani Ungeomba Wewe Ungeulizwa

**2 Wafalme 1 na 2**



BWANA akapenda kumchukua Eliya kuwa naye mbinguni kwa upepo wa kisulisuli. Kazi aliyompa katika kizazi cha uovu, ilikuwa inakaribia kuisha. Alikuwa amepigana kwa ujasiri vita ya BWANA na Mungu alijua atamchukua. Basi Eliya akatoka Gilgali pamoja na Elisha, akamwambia akae akimngoja, maana BWANA amemtuma aende mpaka Betheli. Lakini Elisha akakataa akisema, "Kama BWANA aishivyo, na roho yako iishivyo, sitakuacha," basi wakashuka mpaka Betheli. Wana wa manabii walio Betheli wakamwambia Elisha kama anajua kwamba bwana wake atachukuliwa kwenda mbinguni siku ile, asiwe mkubwa wake? Elisha akasema anajua, wao wanyamaze tu. Eliya akamwambia Elisha tena "kaa hapa … maana BWANA amenituma niende mpaka Yeriko," na Elisha akajibu vile vile, kama alivyojibu wakiwa Gilgali. Basi wakafika Yeriko, wana wa manabii wakamwuliza Elisha tena, kama anajua bwana wake atatatwaliwa asiwe mkubwa wake? Naye akasema anajua. Mara ya tatu pia alimwambia Elisha kaa hapa, "maana BWANA amenituma niende mpaka Yordani." Akajibu vilevile. Wana hamsini wa manabii walisimama karibu yao, na Elisha na Eliya walikuwa ngambo ya Yordani. Eliya

akatwaa vazi lake na kulikunja akayapiga maji, yakagawanyika wakavuka, kama Waisraeli walivyovuka walipotoka Misri. Baada ya kuvuka, Eliya akamwambia Elisha aombe lolote atakalo kabla hajachukuliwa mbinguni na kumwacha. Je, angeomba fedha, nyumba, cheo, au vitu vingine vya kidunia? Basi Elisha akaomba roho ya Eliya maradufu, au mara mbili iwe juu yake. Kuwa na roho hiyo ni kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu. Eliya alimwambia, ameomba neno gumu, lakini akiona ametwaliwa, basi atapata karama hiyo aliyoiomba. Ikawa walipokuwa wakiendelea mbele, na kuongea, tazama kukatokea gari la moto, na farasi wa moto, likawatenga wale wawili, naye Eliya akapanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli. Gari la moto la utukufu wa ajabu na kushangaza. Lugha ya kibinadamu haiwezi kueleza gari la mbinguni linavyofanana, sio benzi wala prado.

Elisha akaona na kulia, "baba yangu, baba yangu, gari la Israeli na wapanda farasi wake." Asimwone tena kabisa; akashika mavazi yake mwenyewe na kuyaraua vipande viwili. Kisha akaliokota lile vazi la Eliya lililomwangukia, akarudi, akasimama ukingoni mwa Yordani. Akalitwaa lile vazi la Eliya lililomwangukia, akayapiga maji, akisema, "Yuko wapi BWANA, Mungu wa Eliya? Naye alipoyapiga maji ya Yordani yaligawanyika. Elisha akavuka." Wana wa manabii waliokuwako Yeriko wakimkabili walipoona walisema, "Roho ya Eliya inakaa juu ya Elisha." Wakainama kifudifudi mbele zake. Wakamwambia kuna watu 50 hodari waende wakamtafute bwana wako Eliya, labda Roho wa BWANA amemtupa juu ya mlima mmoja au bonde moja. Elisha akijua Mungu amemchukua aliwaambia wasijisumbue. Waliposisitiza, alisema, "Haya watumeni." Walirudi bila kumwona. Akasema "Je! mimi sikuwaambia, msiende?

Wakati Mungu atakuteua kujaza nafasi, atakupa mafunzo, nguvu, na heshima inayohitajika kufanya kazi hiyo kwa utukufu Wake. Swali ni, je! Utabakia katika nafasi yako ya mtumwa kwa uaminifu, ukifanya kazi ya unyenyekevu, hadi Mungu atakapoona inafaa sasa kukupa wewe majukumu makubwa? Wakati umepokezwa kijiti cha mbio au vazi, je! Utakichukua kwa imani na ujasiri? Je! Utauona "Mto wa Yordani" kama fursa, au kikwazo?

Mungu bado yuko tayari kuitenganisha Yordani, kuyaponya maji, na kutetea wafanyikazi Wake. Mungu haachi kazi Yake wakati kiongozi mkubwa anastaafu. Kadiri tunavyojitoa Bwana atatatusaidia kupokea Roho Mtakatifu ambaye atatuwezesha kufanya matumizi ya ya taaluma ya kufundisha Wainjilisti wengine kuwa bora zaidi. Nguvu hiyo bado inapatikana leo. Wacha tuiulizie, nasi tutapewa maradufu. Maradufu ya nguvu ya Roho Mtakatifu watapewa wale tu ambao wataendelea kwa uaminifu kuambatana na Mungu kama Elisha alivyokuwa akifanya kwa Eliya. Wacha Baba yetu wa Mbinguni atusaidie kila siku kuwa na njaa na kiu ya Neno Lake, ili tuishi kikamilifu katika mapenzi ya Roho Wake! Ombi: Nisaidie kusulubisha nafsi na kufanya kazi yako bila kujali kukosolewa, kukatishwa tamaa, upinzani na kutoa machozi. Nikumbushe kuwa Wewe Bwana, unasimamia kazi yangu. Nisaidie kukutazama tu, na kufanya kile unachoniuliza kufanya. Acha niwe mwaminifu kama Elisha, katika huduma Yako.

Wazazi wana jukumu kubwa hakika kuwasaidia watoto wao kuwa kama Elisha. Naomba iwe matamanio ya wazazi wao kumpenda na kumjua Yesu huku wakishikilia mkono wa Mungu. Watoto uangalia mifano kila wakati; Wataiga mapema au baadaye. Kwa hivyo, kila wakati tutafute kumwiga Kristo, Ili watoto wanapotuiga, wawe wanamwiga Kristo. Wakristo wengi wanataka kuwa kwenye kizazi cha mwisho ili wasione kifo. Tunaambiwa hiyo sio heshima au nyadhifa kubwa zaidi ambayo Mungu anaweza kumpa mtoto Wake. Nyadhifa ya hali ya juu zaidi ni "ushirika na Kristo katika mateso Yake." Bila kuyakaribisha mateso yasiyofaa. Hii itakuja kwa mtu yeyote anayeishi maisha yaliyoelezwa hapa: Hitaji kubwa zaidi la ulimwengu ni watu- watu ambao hawatanunuliwa wala kuuzwa, watu ambao katika roho zao za ndani ni wakweli na waaminifu, watu ambao hawaogopi kuiita dhambi kwa jina lake halisi, watu ambao dhamiri yao ni ya kiukweli kwa jukumu kama vile sindano ya dira ilivyo, watu ambao watasimamia haki kwa ujasiri, hata mbingu zikianguka. Mateso yasiyoweza kuepukika yanatokana na kuishi maisha ya aina hii 2 Timotheo 3:12. Hii ndiyo heshima ya juu zaidi ambayo Mungu anaweza kumpa binadamu yeyote!

Maandiko yanatuambia kuwa ni watu wawili waliochukuliwa mbinguni bila kuonja mauti, nao ni Henoko na Eliya. Hawa wanawakilisha watu watakaoingia mbinguni bila kuonja mauti Yesu atakaporudi. Na Musa anawakilisha walioonja mauti na kuchukuliwa mbinguni. Ahadi ya ushindi imetolewa kwa wote, na ikiwa tutakuwa waaminifu, siku moja tutamuona Eliya na Musa kule mbinguni.

*Mara nyingi kuna hatari ya kukosea hapa. Kwa kuamini kwamba wataponywa katika jibu la maombi, wengine wanaogopa kufanya chochote kile ambacho kinaweza kuonekana kwamba kinaashiria ukosefu wa imani kwa upande wao. Lakini hawapaswi kupuuza kuyaweka mambo yao sawa kama wanavyotamani kufanya ikiwa kuna tarajio la wao kuondolewa kwa kifo. Wala hawapaswi kuogopa kusema maneno ya kutia moyo au ushauri ambao wangetamani kuuotoa katika saa ya kuagana kwa wapendwa wao.


---

Ni nini kilikuwa kinaenda kutokea kwa Eliya? Elisha alijisikiaje? Kwa nini Elisha hakumwacha Eliya? Hili linaonesha nini kuhusu Elisha? Elisha aliomba apewe nini? Je, unafikiri hili lilikuwa jambo jema kuomba? Je, Elisha alimwona Eliya akichukuliwa?

**SIKU YA 128**
**(Mei 7)**

# Watoto Wakorofi Waadhibiwa

**- 2 Wafalme 2-3**



Elisha alirejea baada ya Eliya kutwaliwa. Watu wa mjini wakamwambia, mahali hapa ni pazuri ila maji hayafai na nchi huzaa mapooza, akasema walete chombo kipya, na watie chumvi ndani yake. Wakamletea na akatoka na kwenda kwenye chemchemi hiyo na kutupa chumvi humo, akisema BWANA asema, “nimeyaponya maji haya, hakutatoka huko tena kufa wala kupooza.” Maji yale yakapona. Elisha akakwea kwenda Betheli na vijana wakorofi, wenye mzaha wakawa wanaimba kwa nabii huyu, “paa wewe mwenye upaa!” Wakimaanisha naye aende mbinguni. Kumbe watu walikuwa wamesikia kupaa kwa bwana wake Eliya, ila hawakuamini bali walitaka wafanye mzaha na mambo ya mbingu. Elisha aliona hawa wanataka kuharibu kazi kubwa aliyoipokea na kumfanya kichekesho fulani. Hata hivyo alishangaa kwamba tukio la zawadi kubwa ya kuingia mbinguni kwa bwana wake kwa shangwe liwe la kukejeliwa. Basi aliwatazama wale watoto na kuwalaani kwa jina la BWANA. Wakaja dubu wawili wa kike toka mwituni na kuwararua vijana 42 miongoni mwao. Kisha akaenda mlima wa Karmeli, na kurudi Samaria. Hatujui kuwa waliumizwa kiasi gani watoto hawa wa mizaha, ila yawezekana walikufa, maana waliraruliwa, pia tunachojua, ni kuwa upuuzi wao au kukosa adabu kwao kulikuwa fundisho tosha kwa vijana au watoto wengine. Wasingeweza kumcheka tena mtumishi mwingine wa Mungu. Hata leo tujihadhari kuwadharau watu wanaomfanyia kazi Mungu, maana wanamwakilisha Yeye, hebu tujitoe kwenye madhara. Kukosea watu heshima hata wa rika lako ni dhambi, Maandiko yanatuamika katika Waefeso 4 kwamba “Maneno mabaya hata yasisikike kamwe miongoni mwenu; kila mara maneno yenu yawe ya kufaa na ambayo hujenga na kuwasaidia wengine, ili yawaneemeshe wasikilizaji wenu. Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu maana Roho huyo ni alama ya Mungu kwenu kwamba ninyi ni watu wake, na thibitisho kwamba siku itakuja ambapo Mungu atawakomboeni. Basi, achaneni na uhasama, chuki, hasira, kelele, matusi! Achaneni na kila uovu! Muwe na moyo mwema na wenye kuhurumiana; kila mmoja na amsamehe mwenzake kama naye Mungu alivyowasamehe ninyi kwa njia ya Kristo”.

Yoramu mwana wa Ahabu alianza kutawala Samaria, mwaka wa 18 wa mfalme

Yehoshafati wa Yuda, na akatawala miaka 12. Akafanya maovu kama babaye machoni pa BWANA. Basi Mesha mfalme wa Moabu aliyekuwa mfuga kondoo akimlipa mfalme wa Israeli sufu ya kondoo 200,000, aliacha wakati Ahabu alipokufa. Ndipo Yoramu akawahesabu Israeli kule Samaria ili waende Moabu, na kutuma ujumbe kwa Yehoshafati amsindikize kwenda kupigana na Moabu. Basi Yehoshafati alikwenda naye kwa njia ya jangwa la Edomu na huko mfalme wa Edomu akajiunga nao. Yehoshafati alimsindikiza akisema, "Nitakwenda, mimi ni kama wewe, watu wangu ni kama watu wako, na farasi wangu ni kama farasi wako." Wakazunguka siku saba, wala hapakuwa na maji kwa mifugo wala watu. Ndipo Yoramu akasema, "Ole wetu! Kwani BWANA amewakutanisha hawa wafalme watatu, awaue mikononi mwa Moabu." Ndipo Yehoshafati akauliza tena kama hapana nabii wa BWANA wamwulize. Mtumishi mmoja wa mfalme wa Israeli Yoramu akasema, Yupo Elisha aliyekuwa mtumishi wa Eliya. Basi wafalme hawa watatu wa Israeli, Yuda na Edomu wakamshukia Elisha, naye akamwambia Yoramu, "Nina nini mimi nawe, uende kwa manabii wa babayo na mamayo. Mfalme wa Israeli akamwambia, La, sivyo; kwa kuwa BWANA amewakutanisha hawa wafalme watatu, awaue mkononi mwa Moabu." Naye Elisha akasema ni kwa ajili tu ya Yehoshafati, mfalme wa Yuda, atawapa heshima, maana ni mcha Mungu, ila kama ni wao wawili, asingewaangalia hata machoni wala kuonana nao. Akaomba aletewe mpiga kinanda, na alipokipiga mkono wa BWANA ukamjia na akasema, "Fanyeni bonde hili lijae mahandaki. Kwa kuwa BWANA asema hivi, hamtauona upepo, wala hamtaiona mvua, ila bonde hilo litajaa maji; nanyi mtakunywa, ninyi, na ng'ombe zenu na wanyama wenu." Akawaambia jambo hili ni jepesi machoni pa BWANA; pia atawatia Wamoabi mikononi mwao, nao watapiga kila mji ulio mzuri, na kila mti mwema mtaukata, na chemchemi zote za maji watazizba, na kila mahali palipo pema watapaharibu kwa mawe.

Ikawa asubuhi, wakati wa kutoa sadaka, maji yakaja hata nchi ikajaa maji. Wamoabi waliposikia wafalme watatu wamekwea ili kupigana nao, walijikusanya pamoja, wote wawezao kuvaa silaha na wenye umri zaidi wakasimama mpakani. Asubuhi, jua likametameta juu ya maji, mifugo na watu wakanywa. Lakini Wamoabi kwa upande wao waliona damu juu ya yale maji, na wakasema bila shaka hao wafalme wameharibika, wamepigana wao kwa wao na kila mtu na mwenziwe, basi wakaambiana waende kuchukua nyara. Walipokuja kwa Israeli Wamoabi walipigwa mpaka kwao. Waisraeli wakabomoa ile miji na wakatupa katika kila mahali palipo pema kila mtu jiwe lake, wakapajaza. Wakaziba chemchemi na kukata miti yote mizuri na kukusanya mawe na wenye kombeo wakatembea wakiupiga mji. Mfalme wa Moabu alipoona ameshindwa alichukua watu 700 wenye kufuta panga ili waende hata kwa mfalme wa Edomu, lakini hawakudiriki, ndipo alipotoa sadaka ya kuteketezwa ya mwanawe wa kwanza ambaye alikuwa mrithi wa ufalme. Kukawa hasira kuu juu ya Israeli, wakatoka wakarudi makwao. Machimbo ya siku za karibuni Moabu yameonesha bango lililoandikwa vita hii. Neno la Mungu ni la kweli siku zote, tunaweza kuwa na mashaka, ila mwishowe tutagundua ni kweli. Ni rahisi kwa Mungu kutupa mahitaji yetu ya kimwili. Lakini Anafurahia kufanya zaidi ya hayo. Anaahidi mwongozo, ukombozi, na ushindi kwa wale wanaomtafuta. Mungu anapofunua njia ya kutokea, huenda ikaonekana kuwa haiwezekani kwa mawazo yetu ya kibinadamu ila Yeye ana nguvu zote. Maisha ya Kikristo ni vita

na gwaride kali na siyo lelemama. Lakini ushindi unaopatikana haupatikani kwa nguvu za kibinadamu. Mioyo yetu ndiyo uwanja wa vita. Soma waefeso Sita kuhusu kuvaa silaha za vita. Vita ambayo inatupasa tupigane— ni vita kubwa zaidi ambayo imewahi kupiganwa na wanadamu—ni kuitoa nafsi kwa mapenzi ya Mungu, kuutoa moyo kikamilifu. Mtu wa kale lazima azaliwe upya kwa maji na damu na kuacha tamaa za mwili, la sivyo hatuwezi kuurithi ufalme wa Mungu. Mielekeo ya urithi, tabia za zamani, au mapokeo lazima viachwe.

Wale wanaoamua kuingia katika ufalme wa kiroho watapata kwamba nguvu zote na tamaa za asili, zisizozaliwa upya, zikiungwa mkono na nguvu za ufalme wa giza, na kulengwa dhidi yao. Ubinafsi na kiburi vitapinga kitu chochote ambacho kingewaonyesha dhambi yao. Sisi wenyewe hatuwezi kushinda tamaa mbaya na tabia ambazo zinajitahidi kuota mapembe mioyoni mwetu. Hatuwezi kumshinda adui mwenye nguvu ambaye anatushikilia katika misukumo yake. Mungu pekee Yake Ndiye anayeweza kutupa ushindi. Anatutaka tuamue kwa mapenzi yetu wenyewe. Yeye hatulazimishi kushirikiana Naye, japo anapenda kufanya hivyo. Roho wa Mungu hufanya kazi kupitia uwezo na nguvu tulizopewa. Nguvu zetu zinahitajika ili kushirikiana na Mungu. Unapokabiliwa na shida, jibu lako la kwanza ni lipi? Chagua imani ambayo inaweza kuleta maji jangwani kukuokoa kutoka kwa majeshi ya Shetani.

*Lakini baada ya kuwaombea kwa bidii wagonjwa nini kifuate basi? Je, ninaacha kufanya yote niwezayo kwa ajili ya kupona kwao?—Hapana, ninafanya kazi kwa bidii zaidi, kwa maombi mengi kwamba Bwana apate kubariki njia ambayo mkono Wake Mwenyewe umetoa; ili aweze kutoa hekima iliyotakaswa kwa ajili ya kushirikiana Naye katika kuwaponya wagonjwa.

*Matibabu ya Dawa Yanapaswa Kutumiwa Pamoja na Maombi ya Uponyaji— Wale wanaotafuta uponyaji kwa maombi hawapaswi kupuuza kutumia tiba rahisi (au tiba mbadala) ambayo ipo karibu nao, na wanaweza kuipata kwa urahisi, nayo ikawa na matokeo mazuri tu. Kutumia tiba zile ambazo MUNGU amezitoa katika kupunguza maumivu na kusaidia asili/mwili katika kazi yake ya urejeshaji afya sio kuikana imani. Kushirikiana na MUNGU, na kujiweka katika hali rafiki inayoleta uponyaji siyo kukana imani. MUNGU ameweka ndani ya uwezo/uwezekano wa kujipatia ujuzi wa sheria za uhai/uzima. Maarifa haya yamewekwa ndani ya maeneo yetu ya karibu, ili tuweze kuyafikia, kwaajili ya matumizi/kuyatumia. Tunapaswa kutumia kila miundombinu kwaajili ya urejeshaji wa afya, tukitumia kila fursa inayowezekana, kwa kufanya kazi kwa kulingana na sheria za asili. Wakati tumesali ili wagonjwa wapone, tunaweza kufanya kazi kwa nguvu nyingi zaidi, tukimshukuru MUNGU kwamba tunao upendeleo wa kushirikiana Naye, na kuomba baraka Zake juu ya njia ambazo Yeye Mwenyewe ametuandalia/ametujalia.

---

Elisha aliishi wapi? Alisaidiaje maji kuacha mapooza? Kwa nini vijana 42 waliraruliwa na dubu? Elisha aliishi wapi? Kwa nini wafalme watatu walimuita Elisha? Elisha aliwaambiaje?

**SIKU YA 129**
**(Mei 8)**

# Mwanamke Mjane na Mafuta na Mwanamke Mshunemu

**- 2 Wafalme 4-6**



Sehemu nyingi za Israeli watu walisikiliza mafundisho ya Elisha na manabii na kumwabudu Mungu. Elisha aliendа huko na huko akikutana na watu, na kuwafundisha kumwabudu Mungu wa kweli. Basi mwanamke mmoja miongoni mwa wake za wana wa manabii alimlilia Elisha akisema, "Mtumishi wako mume wangu amekufa; nawe unajua mtumishi wako alikuwa mcha BWANA; na aliyemwia amekuja ili ajitwalie wana wangu wawili kuwa watumwa." Siku hizo, na hata siku hizi, katika baadhi ya maeneo, watu wengine wanachukua watoto wa mtu kama rehani kama asipolipa deni. Jambo hili lilikuwa chungu, maana alikuwa amefiwa na mume, na sasa watoto wanachukuliwa kuwa watumwa. Elisha akamwambia kwa huruma "nikufanyie nini?" BWANA anapenda kutusaidia katika shida zetu. Basi, Elisha alimwambia yule mwanamke, ana nini kwake. Naye akasema hana kitu chochote ila chupa ya mafuta. Akamwambia aende na kuazima vyombo vingi kwa majirani zake. Kisha aingine ndani na kujifungia na wanawe. Akamimine mafuta kwenye vyombo vyote, navyo vilivyojaa avitenge. Mama huyu alifanya hivyo na wanawe, naamini watoto hawa walipata mshangao na wakajua kuwa BWANA anawapenda na ana mpango nao. Bila shaka watu walishangaa wanaazima vyombo vyote vya nini, au ni kuchanganyikiwa baada ya kufikwa na madeni? Basi walijifungia, mama yule akamimina mafuta kidogo kidogo kwa kila chombo, na akimimina tu yanajaa kwenye chombo, akawaambia wanawe waendelee kuleta vyombo vingine, na ndipo waliposema "vyombo vyote vimekwisha." Pengine baada ya muda na majirani walikuja kushuhudia. Mama huyu akaenda kumwambia nabii Elisha akitabasamu, naye akamwambia akayauze mafuta hayo na kulipa deni lake, na yale mafuta yaliyosalia, "uyatumie wewe na watoto wako." Kadiri ya imani na vyombo vyake akapokea.

Siku moja alipokuwa akienda Shunemu, alikutana na mwanamke mmoja mwenye madaraka makubwa, huyu akamkaribisha nyumbani kwake kwa chakula. Basi Elisha kila alipopita njia hiyo alienda kukaa na familia ya mama huyu wa Shunemu na mume wake. Mwishowe yule mama alimwambia mume wake, "naona ya kuwa

mtu huyu apitaye kwetu mara kwa mara ni mtu mtakatifu wa Mungu." Akamwomba mumewe wamfanyie chumba kidogo ukutani na ndani yake waweke kitanda, meza, kiti na taa, ili anapowatembelea, afikie humo. Hili ni jambo jema, wengi huongeza nyumba zao kwa ajili ya tamaa, fahari au kuongeza anasa, lakini hii familia iliongeza nyumba ili kukarimu wageni.

Siku moja Elisha alipowatembelea, kabla hawajaondoka, akamwambia mtumishi wake, Gehazi, amwite huyu mama Mshunami. Gehazi alimwita, naye Elisha akamwambia, "Tazama wewe umetutunza namna hii, je, utendewe nini basi? Je! uombewe neno kwa mfalme, au kwa amiri wa jeshi?" Yule mwanamke akajibu kwa kuridhika, kwamba anakaa na watu wake wala hana shida. Basi alimwuliza Gehazi apeleleze naye akagundua kuwa yule mama na mumewe hawakujaliwa mtoto. Basi alimwita tena yule mama, naye akasimama mlangoni, ndipo Elisha akasema, "Panapo wakati huu mwakani, utamkumbatia mwana." Yule mama akasema, "La! Bwana wangu, wewe mtu wa Mungu, usiniambie mimi mjakazi wako uongo." Maana alikuwa na shauku ya kuwa na mtoto, ila aliogopa matumaini yake yanaweza kuja juu na asipate mtoto. Basi yule mwanamke alichukua mimba, na kuzaa mwaka uliofuata, kama Elisha alivyosema.

Mtoto alikua na siku moja alipoenda shambani kuvuna na babaye, akamwambia baba yake, "kichwa changu, kichwa changu." Ndipo babaye akamwambia mtumishi ampeleke mtoto kwa mama yake. Alipochukuliwa kwa mamaye hali ilibadilika, akawa amezidiwa ugonjwa, kisha jioni akafa. Mamaye akapanda juu, na kumlaza mtoto kwenye kitanda cha Elisha na kufunga mlango, akamwita mumewe ampe mtumishi mmoja ili amwendee yule mtu wa Mungu kwa haraka (maana Elisha na Gehazi walikuwa wameondoka). Hakumwambia mumewe sababu ya kutaka kumfata Elisha. Mumewe akashangaa mbona anaenda wakati ule na siyo siku maalumu ya mwezi au Sabato. Yule mama akasema haidhuru neno. Mama akatandika punda na kumwambia mtumishi wake waende haraka, asipunguze mwendo kama hakumwambia. Wakafika kwa Elisha mtumishi wa Mungu huko Karmeli, na Gehazi akamwona na kumwambia Elisha mtu anayekuja. Akamwambia Gehazi aende kumwuliza kama mambo yote ya familia yake yako sawa - mume na mtoto na wote hawajambo? Yule mama alisema yote ni sawa. Alipofika kilimani, ndipo alimshika miguu Elisha. Gehazi akataka amwondoe, lakini Elisha akamkataza, "mwache maana roho yake ndani yake ina uchungu na BWANA amenificha, wala hakuniambia."

Ndipo yule mwanamke Mshunami akasema, "Je! niliomba mtoto kwa bwana wangu? mimi sikusema usinidanganye?" Ndipo Elisha akamwambia Gehazi ajikaze na kwenda na fimbo yake mkononi, na akikutana na mtu asimsalimu au kujibu, kisha aweke fimbo juu ya uso wa mtoto. Mama huyu akasema hatamwacha Elisha na kwenda mwenyewe, basi Gehazi akatangulia naye akafuata na Elisha. Gehazi alipoweka fimbo kwenye uso wa mtoto, hakukuwa na sauti wala majibu, akaenda kumwambia Elisha, "mtoto hakuamka." Basi Elisha alipofika na kukuta mtoto amelazwa kitandani akajifungia mlango yeye na yule mtoto na kumwomba BWANA. Akapanda kitandani na kujilaza juu ya mtoto, akaweka kinywa chake juu ya kinywa cha mtoto na macho yake juu ya macho ya mtoto na mikono yake juu ya

mikono ya mtoto. Akajinyosha juu ya mwili wake, na mwili wake yule mtoto ukaanza kupata moto. Elisha akatembea na kurudi tena kujinyosha juu ya mtoto, mara mtoto akapiga chafya mara saba na kufumbua macho yake. Akamwita Gehazi amwite yule mama Mshunami, na alipofika alimwambia amchukue mtoto wake. Mama yule alianguka chini ya miguu ya Elisha, kisha akamchukua mwanawe na kutoka. Mungu ana zawadi kwa wale wanaohudimia watumishi wake waaminifu. Mama yule alipokea zawadi hizo.



Mtoto huyu aliona mfano mzuri na wa thamani kubwa. Siku hizi watoto wengi huwapa heshima wacheza filamu, wachezaji michezo ya kulipwa na watu ambao wako kwenye fasheni. Hili ni kosa, tunapaswa kuheshimu na kuweka thamani kwa wacha Mungu. Mtoto huyu alijifunza kuomba, na kutafakari Neno la Mungu kutokana na ushuhuda mkuu wa maisha yake.

*Mtumaini MUNGU bila kujali Matokeo Ya Maombi Yatakuwaje-Tunapoomba kwa ajili ya kupona kwa wagonjwa, haijalishi matokeo ya jambo hilo, hebu tusipoteze imani kwa MUNGU. Ikiwa tutaitwa kukutana na msiba, hebu tukubali kikombe chenye uchungu, tukikumbuka kwamba mkono wa Baba unakishikilia kwenye midomo yetu. Lakini ikiwa afya itarejeshwa, haipaswi kusahaulika kwamba mpokeaji wa rehema ya uponyaji anawekwa chini ya wajibu uliofanywa upya kwa Muumba.

---

Elisha alimsaidiaje yule mwanamke mjane? Huyo mjane alikuwa na watoto wangapi? Kwa nini mtumishi wa Elisha hakuweza kumfufua mtoto? Kwa nini Elisha alitaka kumpa zawadi mama Mshunami?

**SIKU YA 130**
**(Mei 9)**

# Chakula Chenye Sumu na Shoka Lililozama

**- 2 Wafalme 4-6**

Wakati huu wa shida nyingi na giza, Mungu alijitokeza na kuwasaidia watu Wake kwa miujiza mingi. Basi Elisha akafika Gilgali tena, na kulikuwa na njaa katika nchi na hao wana wa manabii walikuwa wakikaa mbele yake kwenye shule za manabii. Naye Elisha aliwaambia watumishi wake aweke sufuria kubwa ili awapikie hawa wana wa manabii. Na mmoja wao akaenda nje kondeni ili kuchuma mboga, akaona mtango mwitu, na kuyachuma, hata nguo yake ilikuwa imejaa. Akaja na kuyapasua kisha akayaweka sufuriani, japo hawakuyajua kama yanaliwa au la. Hata siku hizi kuna uyoga na mimea isiyoliwa, hivyo peleleza kwa wataalamu ni mimea gani inayoliwa na isiyoliwa maana wakati wa dharura utafaidika. Basi wakawapakulia wale wana wa manabii na walipokuwa wanataka kula chakula, wakapiga kelele, "Ee mtu wa Mungu mauti imo sufuriani" wakimaanisha matango yale ni sumu, si ya kuliwa na watu. Wala hawakuweza kuendelea kula. Elisha akawaambia walete unga, naye akautupa ndani ya sufuria na kuwaambia wapakulie watu ili wale. Sumu yote ilitoka, kikawa chakula kizuri tu kwani Mungu aliondoa kitu kibaya sufuriani. BWANA alisikia maombi ya mtu wa Mungu na kuikata sumu. Hata leo tunaweza kuomba kwa imani, endapo tumeingia shidani, kwa kutojua, au hata kwa kujua.

Wakati huo huo wa njaa akaja mtu kutoka Baal-shalisha, akamletea mtu wa Mungu chakula cha malimbuko, mikate ishirini ya shayiri na masuke mabichi ya ngano guniani, akasema wape watu wale. Mtumishi wa Elisha akashangaa, chakula kidogo hiki awape watu mia? Ila Elisha akasema uwape watu wale "kwa kuwa BWANA asema hivi, watakula na kusaza." Akawaandalia, nao wakala na kusaza sawasawa na Neno la BWANA.

Basi wana wa manabii walikuwa wengi, wakitaka kusoma ili wamfanyie kazi BWANA. Shule kama hii leo inaitwa shule ya umishonari, au shule ya huduma au seminari. Basi walimjia Elisha na kusema, Tukaapo mbele yako ni padogo kwetu. Wakamwomba waende Yordani na kutwaa mti kila mmoja, ili wajifanyie mahali pa kukaa. Elisha akajibu, haya. Mwanafunzi wa mmoja akamsihi aende nao, akasema nitakwenda. Basi wakaenda kule na walipofika, wakakata miti. Lakini mmojawapo alipokuwa katika kukata boriti, chuma cha shoka kikaanguka majini. Ndipo akalia akisema, "Ole wangu! Bwana wangu, kwani kiliazimwa kile." Elisha akauliza, kilianguka wapi? Naye akamwonyesha, ndipo Elisha alipokata kijiti na akakitupa pale pale, chuma kile kikaelea, akamwambia yule mwanafunzi wa shule ya manabii, "kiokote", naye akanyosha mkono akakitwaa. Bila shaka yule mwanafunzi alishukuru kuwa pamoja na mtu wa Mungu na kusaidiwa.

Hata leo, wale wanaosomea uchungaji au uinjilisti ili waongoze watu wanapata

shida mbalimbali wanapokuwa chuoni au wanapotafuta njia za kuanza kozi. Lakini kwa mfano huu, jua kwamba utakapopata wito wa kumfanyia Mungu kazi kwa kuhudumia watu, yeye atakuwa nawe daima. Basi, jifunze maisha ya kuridhika na utauwa, kwani kazi ya kumtumikia Mungu si ya 'kutengeneza pesa,' bali ni ya kutengeneza tabia ya mbinguni, kwako binafsi na kwa wengine. Hiyo ukiifanya inavyotakwia, ni ya kujinyima. Mifano ya Biblia haioneshi watumishi wa Mungu wakiishi maisha ya kuwa na pesa nyingi, madeni tele au kuwa waombaji kwa watu ili wawape pesa ndipo wawabariki. Kuwa tajiri si tu kuwa na pesa, bali kuwa na mahitaji machache maana unajifunza kuridhika katika hali zote, kwani utauwa na kuridhika ni faida kubwa. Utayaweza mambo yote kwake yeye akutiaye nguvu Filipi 4:13. Yeye ameahidi kuwa hatakuacha. Usijilinganishe na jirani kama ana nyumba kubwa kupita yenu, au shamba kubwa au pikipiki nzuri kupita yenu. Kita kuangalia baraka ulizonazo, siyo zile usizonazo, zihesabu, na kisha msifu Mungu. Utaona uso wako uliokunjamana unapata furaha. Utamaduni wa leo ni kwamba furaha inapatikana kwa vitu. Je, inakuwaje watu wanahuzunika wakikaa na mtu mwenye tamaa ya vitu! Jambo jiningi la kuona hapa ni kuhusu mkopo au deni, Kwenye Maandiko, mambo ya kuchukua mkopo yametajwa mara 26 na mara zote ni hasi.

Mara zingine ni muhimu kuazima au kuchuka mkopo, ila yabidi tuepuke tunavyoweza, na tumwombe Mungu tuweze kuishi maisha ya kiasi, na kujikimu na vifaa muhimu kama jembe, ndoo, sufuria, shoka n.k. Baraka nyingi tulizonazo ni kama ifuatayo:

1. Kama leo hii umeamka na afya bila ugonjwa, au hujafa bado, basi umebarikiwa kuliko watu zaidi ya laki moja wanaokufa kila siku.

2. Kama unaishi pasipo na vita au njaa, una bahati zaidi ya watu milioni 500 wanaoishi sehemu zenye mapigano na mateso.

3. Kama unaishi mahali ambapo kuna uhuru wa kuabudu bila ya kuhatarisha usalama wako, basi umebarikiwa kuliko watu bilioni 3 ambao ni nusu ya dunia. Hawa hawana uhuru kamili wa kuabudu katika nchi zao.

4. Kama una nguo za kuvaa, chakula, nyumba ya kulala, na kitanda, basi, umebarikiwa kuliko asilimia 75 ya watu wote duniani.

5. Kama una pesa benki, na chenji chenji kwenye sahani, au mahali fulani nyumbani, basi wewe ni kati ya asilimia 8 ya watu duniani ambao mna uwezo huo.

6 Kama una wazazi wote wawili, umebarikiwa kuliko wengi ambao ni yatima au wana mzazi mmoja.

7. Kama wazazi wako wana Shahada ya elimu, basi umebarikiwa kuliko asilimia 99 ya watu ambao hawana shahada yoyote duniani.

8. Na mwisho, kama umeweza kusoma tuliyoandika hapa, umebarikiwa kuliko watu zaidi ya bilioni mbili duniani, ambao hawawezi kusoma wala kuandika.

*Ombi la Msamaha Daima Hujibiwa haraka yaani papo hapo—Tunapoomba baraka za kidunia, jibu la ombi letu linaweza kucheleweshwa, au MUNGU anaweza kutupa kitu kingine tofauti na tunachoomba, lakini si hivyo tunapoomba ukombozi kutoka katika dhambi. Ni mapenzi Yake kutusafisha dhambi, kutufanya sisi watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Masihi "alijitoa nafsi Yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atukomboe na ulimwengu huu mbovu wa sasa, kama yalivyo mapenzi ya MUNGU Baba yetu." Wagalatia 1:4. "Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu chochote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye anatusikia; na kama tukijua ya kuwa anatusikia, tuombalo lo lote, twajua ya kuwa tunazo haja tulizoziomba Kwake." 1 Yohana 5:14, 15. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni Mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. 1 Yohana 1:9.

---

Kwa nini wana wa manabii walikata miti? Chuma cha shoka kilipatikanaje? Kwa nini chuma hakielei? Kwa nini walilia kuwa maiti imo sufuriani? Kisa hiki kinatupatia mafundisho gani? Hesabu baraka zako zote na uziandike. Kisha hesabu yote mabaya au usiyo nayo na uyaandike.

**SIKU YA 131**
**(Mei 10)**

# Jemedari Naamani na Mjakazi Mtumwa

**- Zawadi za Mungu haziuzwi 2 Wafalme 5**

Naamani, jemedari wa jeshi la mfalme wa Shamu au Syria, alikuwa mtu mwenye cheo, na wa kuheshimiwa mbele ya bwana wake, kwa vile kwa mkono wake BWANA alikuwa amewapa Washami kushinda. Alikuwa mtu hodari wa vita, lakini alikuwa na ukoma. Washami walikuwa wameteka nyara kule Israeli na kuchukua mtoto wa kike ambaye alichukuliwa na kuwa mfanyakazi wa ndani wa Naamani. Ilikuwa ni ukatili kwa msichana huyu kuchukuliwa mateka na kwenda mbali na kwao, asiwaone wazazi au nduguze. Msichana huyu alimwabudu Mungu wa mbinguni, alikuwa na upendo, japo aliishi utumwani huko Syria. Inaonekana tajiri yake, mama mwenye nyumba, alikuwa ni mtu mwenye roho nzuri, na walikaa wakazungumza kama mama na binti yake. Mara zingine huyu bosi wake, alionekana mwenye huzuni na kusononeka. Bila shaka, ni kwa sababu ya shida ya mume wake Jemedari aliyekuwa ugonjwa wa ukoma.  Msichana huyu mateka, alieleza visa vya Elisha, nabii wa Mungu, kama vya kufufua wafu, kufanya chakula cha sumu kiweze kuliwa n.k. Haijalishi umri wako ni upi, unaweza kuwa mtu wa kupeleka habari njema kwa wale walio wagonjwa, masikini, wenye shida au wenye huzuni.

Akamwambia mke wa Naamani, “Laiti bwana wangu angekuwa pamoja na yule nabii aliyeko Samaria, maana angemponya ukoma wake.” Alikuwa ana maana nabii Elisha, basi mtu mmoja aliyesikia, alieleza hayo kwa Naamani, na Naamani akamwambia mfalme wa Shamu. Mfalme akafurahi kwamba yule anayemsaidia



katika jeshi lake, atapata matibabu ya ugonjwa mbaya na mgumu kupona. Akamwambia atampa barua ya kumtambulisha kwa mfalme mwenzake kule Israeli, ili amsaidie, aponywe ukoma. Naamani akaenda zake Israeli akichukua talanta kumi za fedha, vipande vya dhahabu na vya fedha na mavazi kumi. Akampa Naamani ule waraka, na kusema nimetuma mtumishi wangu Naamani kwako. Yule Mfalme wa Israeli alipopata ile barua, akakasirika sana, akaona kama anachezewa au anatafutwa ugomvi na mfalme wa Shamu. Mfalme wa Israeli alirarua mavazi yake na kusema, "Je! mimi ni Mungu niue au kuponya, hata mtu huyu akanipelekea mtu nimponye ukoma wake? Fahamuni basi, nakusihini, mwone ya kuwa mtu huyu anataka kugombana nami."

Ikawa Elisha nabii aliposikia kwamba mfalme wa Israeli ameyararua mavazi yake, ndipo akatuma mtu kwa mfalme akisema, "mbona umeyararua mavazi yako? Na aje sasa kwangu mimi, naye atajua ya kuwa yuko nabii katika Israeli." Basi Naamani akaja na farasi wake na magari yake, akasimama mlangoni pa nyumba ya Elisha. Elisha akapekea mjumbe akimwagiza amwambie "Enenda ukaoge katika Yordani mara saba, na nyama ya mwili wako itakurudia, nawe utakuwa safi." Lakini Naamani akakasirika, kwani alikuwa ni mtu mwenye cheo na jemadari wa jeshi, japo alikuwa na ukoma. Alikuwa na pembe za kiburi kwa namna fulani. Akasema alifikiri kwamba Elisha atatoka na kuomba kwa Jina la BWANA, Mungu wake, na kupitisha mkono wake mahali penye ugonjwa, na kumponya ukoma wake. Akang'aka, "Abana na Farpari, mito ya Dameski, si bora kuliko maji yote ya Israeli?" Akashangaa kwa nini hawezi kujiosha ndani ya hiyo mito ya nchi yao na kuwa safi. Akageuka kwa hasira ili aondoke. Mungu ashukuriwe, kwani kila mahali, kuna marafiki wenye hekima, na Naamani alikuwa na wenye hekima kati ya watumishi aliosafiri nao. Watumishi wenye hekima wakamkaribia, kwa upole na kwa huruma na kumsihi ajishushe ili akwezwe. Wakasema, "Baba yangu, kama yule nabii angalikuambia kutenda jambo kubwa usingalitenda?" Je, kuna ubaya gani akikwambia jioshe uwe safi? Naamani akaona watumishi wake wamesema maneno ya busara. Akaenda mto wa Yordani unaojulikana kwa maji yenye taka, na kujichovya. Alizama mara moja, na kuona hakuna tofauti, mara mbili, mara tatu, akajiuliza akiendelea, "huku kupiga mbizi kuna faida kweli."

Watu wengi hufikiri wanaweza kufanya mambo kama wapendavyo tu. Mfano, katika kitabu cha Mwanzo 2 tuliagizwa kuwa siku ya saba ni siku ya mapumziko, ni Sabato. Wengi huchukua siku hii kwenda sokoni, kufua nguo zao au kujifanyia kazi zao, wakisema haijalishi siku yoyote tunaweza kumpatia Mungu. Wengine husema muhimu zaidi ni mioyo yetu, na si hizi namba. Mungu ni BWANA mwenye maagizo maalumu. Naamani akaendelea kujizamisha majini, mara ya nne, tano, sita, lakini hakuna kilichotokea, na alipofikisha mara saba ukoma wake ulitoweka, "Nyama ya mwili wake ikawa kama nyama ya mwili wa mtoto mchanga, akawa safi." Alipona ukoma, na makunyanzi yote. Jemadari wa jeshi, mtu wa makamo na 'suluba' nyingi, kuwa na ngozi kama ya mtoto mchanga, ni mwujiza.

Naamani alimrudia mtu wa Mungu, Elisha, na kusimama mbele zake, na akatoa ushuhuda, "Sasa najua ya kwamba hakuna Mungu duniani mwote, ila katika Israeli; basi nakuomba upokee mbaraka kwa mtumwa wako." Kisha akatoa zile zawadi.

Lakini Elisha akakataa kuzipokea kwani uponyaji ulikuwa zawadi toka kwa Mungu, hakutaka uuzwe au ununuliwe. Aliposhurutishwa apokee, alikataa kabisa.
Wengi leo ni kama yule Naamani wa zamani. Wanakataa mambo rahisi ambayo Mungu anawataka wafanye, hasa katika kuzuia magonjwa kwa njia rahisi. Wanaona ni afadhali kutumia pesa kununua dawa wakati ambapo wangekunywa maji nyakati fulani ingesaidia kichwa kupona. Yapaswa tuishi maisha yaliyo sahili na yenye afya kwa kula lishe bora na kuishi mtindo wa maisha ambao Mungu anataka. Wazazi wanapaswa kujitoa kuwafundisha watoto wao kama yule msichana mateka, kwani kwa kiasi kikubwa, hatima ya watoto inaamuliwa na wazazi wao. Kwa hivyo, wazazi, wasilete watoto kwenye ulimwengu huu mbaya kama hawako tayari kuwafundisha njia ya mbinguni. Kuna mbingu ya kujitwalia, na kuzimu kunakopaswa kuepukwa zaidi ya uviko19!

*Mara tu mtoto wa MUNGU anapokaribia Kiti cha Rehema ndipo anakuwa mteja wa Wakili mkuu. Katika tamko lake la kwanza la toba na ombi la msamaha Kristo hutetea kesi yake na kuifanya iwe Yake Mwenyewe, akiwasilisha ombi hilo mbele ya Baba Yake kama ombi Lake Mwenyewe.

---

Naamani alikuwa na ugonjwa gani? Nani alimsaidia? Mfalme wa Shamu alifanya nini kwa Naamani? Kwa nini mfalme wa Israeli aliogopa? Kwa nini Elisha alikuwa tayari kumsaidia Naamani? Kwa nini Naamani alifikiri Elisha hakuwa msaada? Kwa nini Naamani hakurudi? Naamani alikuwaje alipotii?

**SIKU YA 132**
**(Mei 11)**

# Ukoma wa Naamani Wahamia kwa Gehazi

**- 2 Wafalme 5**

Elisha alipokataa kupokea zawadi, Naamani aliomba kuchukua udongo wa Israeli kama zawadi. Akaahidi hatatoa kafara kwa miungu ya kwao tena, isipokuwa kwa BWANA, Mungu wa Israeli. Ila akasema kwamba huwa anamsindikiza mfalme hekaluni kwa mungu wake Rimoni, naye mfalme akiabudu kule, yawezekana, akajitegemeza kwake, naye pia akapiga magoti ili kumtegemeza mfalme asianguke, ila si kwa kuabudu. Elisha akamwambia awe na amani moyoni, naye Naamani akaanza safari ya kurudi. Kabla hajaenda mbali aliona vumbi, kumbe ni Gehazi anamfuatilia kwa nyuma.

Gehazi, mtumishi wa mtu wa Mungu Elisha, aliingiwa na tamaa ya vitu alipoona bosi wake amekataa zawadi za gharama vile. Gehazi alisema, “tazama Elisha amemwachilia Naamani Mshami, asizipokee mikononi mwake hizo zawadi alizozileta”. Akaapa kumfuata mbio, na kupokea vile vitu kwake.

Basi Gehazi akamfuata Naamani. Naye Naamani alipoona anakuja mbio, alishuka garini kwake amlaki, akishangaa akauliza, “Je! ni amani.” Naye Gehazi akasema “ni amani.” Ni kweli vita havikuwepo vya mwili, bali kwenye moyo wake alikuwa na vita vya dhambi ya kutoridhika. Kwa maana utauwa na kuridhika ni faida kubwa. Tulikuja duniani bila kitu na tutaondoka bila kitu. Mungu amekuwa mpaji wa mahitaji yetu tangu uumbaji, kwani aliumba chakula chetu, mianga na kila kitu ndipo akatuumba. Hii ina maana ana mipango ya riziki zetu na hivyo tusiwe na tamaa hata kufanya dhambi. Gehazi akasema uongo kuwa ametumwa na Elisha, kwamba, wana wa manabii wamekuja tu sasa hivi kutoka milima ya Efraimu. Akaomba ampe talanta moja ya fedha na mavazi mawili. Naamani akawa radhi kwa furaha kumpatia kwani alitaka awape vyote mwanzoni, akasema, “uwe radhi ukatwae talanta mbili.” Akamshurutisha Gehazi, na kumfungia talanta mbili, akawatwika watumishi wake wawili nao wakachukua hizo zawadi mbele yake, maana zilikuwa nzito, na ilibidi kuwa na usafiri. Alipofika kilimani akavichukua vile vitu, ili Elisha asimwone, na akaviweka nyumbani mwake, akawaacha wale watu kuondoka, nao wakaenda zao.

Akaingia kusimama mbele ya Elisha, kana kwamba hakuna lililotokea. Ndipo Elisha akamwuliza, “Watoka wapi Gehazi? Akanena, Mtumwa wako hakuenda mahali.” Elisha akamwambia “Je, moyo wangu haukuenda na wewe, hapo alipogeuka yule mtu katika gari ili akulaki?” Yaani, Mungu alimpa maono, aliona gari likigeuka na Naamani akimlaki na akimpatia zawadi. Akamwuliza, “Je, huu ni wakati wa kupokea fedha, na kupokea mavazi, na mashamba ya mizeituni, na mizabibu, na kondoo, na ng’ombe na watumwa na wajakazi?” Kuna wakati wa kupokea vitu, na wakati wa kutopokea!

Elisha akamwambia Gehazi, "Basi ukoma wa Naamani utakushika wewe, na wazao wako hata milele." Gehazi akatoka mbele ya nabii Elisha, akiwa mwenye ukoma kama theluji. Bila shaka hili ni fundisho kwetu kutosema uongo, kutopokea rushwa na kutokuwa na tamaa ya vitu. Mavazi mawili na fedha vilifanya asiwe mrithi wa kazi ya Elisha kama vile Elisha alivyokuwa mrithi wa kazi ya Eliya. Dhambi hii ilikuwa ushuhuda mbaya pia kwani Washami, ambao walihitaji wamjue Mungu wa Ibrahimu, ambaye hauzi uponyaji wake walikwazwa kwa namna fulani kwa kuona kigeugeu cha watenda kazi wa Mungu. Gehazi alimfanya bwana wake aonekane kuwa hana msimamo. Alishuhudia uongo, na uongo ni dhambi.

*Mwambie Yesu mahitaji yako kwa unyofu wa nafsi yako. Hautakiwi kushikilia mdahalo au hoja/mabishano marefu, au kuhubiri mahubiri kwa Mungu, bali kwa moyo wa huzuni kwa ajili ya dhambi zako, sema, "Niokoe, Bwana, la sivyo nitaangamia." Kuna tumaini kwa roho kama hizo. Watatafuta, wataomba, watabisha, na watapata. Wakati Yesu anakapokuwa ameuondoa mzigo wa dhambi unayoiponda nafsi, utapata baraka za amani ya Kristo.

---

Kwa nini Naamani alichukua udongo wa Israeli? Kwa nini Naamani alisema asamehewe akienda kwenye hekalu la Rimoni? Kwa nini Gehazi alipata ukoma? Fundisho gani umepata katika kisa hiki?

**SIKU YA 133**
**(Mei 12)**

# Magari ya Moto

**- 2 Wafalme 6**

Mfalme wa Shamu alipenda kufanya vita na Israeli, na kuwaambia watumishi wake ataweka kituo chake mahali fulani. Yule mtu wa Mungu, Elisha, akapeleka habari kwa mfalme wa Israeli na kusema, "Jihadhari usipite mahali fulani; kwa sababu ndiko wanakoshukia Washami." Mfalme wa Isralelі akapeleka watu mahali pale alipoambiwa, na kutahadharishwa na yule mtu wa Mungu naye akaokoa nafsi yake mara kadhaa. Basi mfalme wa Shamu akafadhaika na kushangaa, kwa ajili ya jambo hili, kwamba siri zake zinavujaje na kwenda kwa jeshi la mfalme wa Israeli? Akaita watumishi wake na kuwauliza kama kuna mmoja wao anawasaliti, au yu upande wa jeshi la Israeli? Wakamwambia La? Hakuna. Akatokea mmoja wa watumishi alimyesaidia kufumbua fumbo au siri. Huyu alimwambia, "Elisha yule nabii aliye katika Israeli humwambia mfalme wa Israeli maneno uyanenayo katika chumba chako cha kulala." Mfalme akasema waende kwa Elisha anapoishi ili wakapeleleze, na watume watu wamkamate. Akaambiwa yupo Dothani. Wakapeleka farasi, magari na jeshi kubwa huko. Wakafika pale usiku, wakauzingira ule mji pande zote. Hata asubuhi na mapema mtumishi wake alipoondoka na kwenda nje, tazama kuna jeshi la watu, farasi na magari yameuzingira ule mji. Akatetemeka akisema, "Ole! Wetu! Bwana wangu, tufanyeje?" Maana walikuwa wamezingirwa.



Elisha akaomba kwa BWANA akisema, "Ee BWANA, nakusihi, mfumbue macho yake, apate kuona." BWANA alifumbua macho ya mtumishi naye akaona kilima chote kilikuwa kimejaa farasi na magari ya moto yaliyomzunguka Elisha pande zote. Elisha akamwomba BWANA alipige lile jeshi kwa upofu. Nao wakapigwa upofu. Elisha akawachukua ili awaongoze akisema, "Njia hii siyo, na mji huu sio, nifuateni mimi, nami nitawapeleka kwa mtu yule mnayemtafuta." Akawapeleka Samaria. Walipokuwa wamefika, ndipo akamwomba BWANA awafumbue macho yao, wapate kuona. "BWANA akawafumbua macho wakaona, kumbe! Walikuwa katikati ya Samaria." Mfalme wa Israeli alipowaona aliomba ruhusa kwa Elisha ili awapige. Elisha akasema hawa ni mateka, ni watumwa wako, uwapigie nini? Wape chakula na maji, kisha watume warudi kwa bwana wao, mfalme wa Shamu, maana watakuwa wainjilisti wa wema na huruma za Mungu. Walipewa maji na chakula tele, na wakaachwa kwenda kwa bwana wao. Hiyo ni dawa kali sana kwa adui; kumtendea wema, kwani hawakuja tena katika nchi ya Israeli. Somo tunalopata hapa ni kuwa tusiwe watu wa kuweka visasi kwa adui zetu, hasa wanapokuwa hawana kitu na ni dhaifu.

Hata nasi leo tunazungukwa na Jeshi la mbinguni. Tukimchagua Mungu kuwa kiongozi wetu, Biblia inasema "Malaika wa Bwana hufanya, akiwazungukia wamchao na kuwaokoa." Basi katika Zaburi tunaambiwa, "Onjeni mwone ya kuwa BWANA yu mwema." Tena, "Nitayainua macho yangu niitazame milima, msaada wangu utatoka wapi?" Anajibu, "Msaada wangu u katika BWANA."

*Tunapoona ubaya wa dhambi, tunaanguka bila msaada mbele ya msalaba, tukiomba msamaha na nguvu, maombi yetu yanasikika na kujibiwa. Wale wanaowasilisha maombi yao kwa MUNGU katika Jina la Kristo hawataachwa kamwe. Bwana asema, "Yeye ajaye Kwangu sitamtupa kamwe." "Atayatazama maombi ya aliye mkiwa." Msaada wa Maombi yetu ya Msamaha unatoka kwa Yeye ambaye anashikilia vitu vyote mikononi Mwake. Amani anayotuma ni uhakikisho wa upendo Wake kwetu.

---

Elisha alikuwa msaada kwa namna gani kwa mfalme wa Israeli? Elisha alijuaje kile Washami walichotaka kufanya? Mfalme wa Shamu alitaka kumfanyia nini Elisha? Mungu alimlindaje? Elisha aliwashinda Washami kwa namna gani?

**SIKU YA 134**
**(Mei 13)**

# BWANA Awapigania Israeli

**- 2 Wafalme 6-7**



Ikawa Ben-hadadi mfalme wa Shamu alikusanya majeshi yake yote akakwea akauzingira Samaria, mji mkuu wa Israeli. Njaa ikawa kuu katika Samaria hata kichwa cha punda kiliuzwa kwa vipande themanini vya fedha, na kibaba cha mavi ya njiwa kikauzwa kwa vipande vitano vya fedha. Hali ilikuwa ngumu, hata mavi ya njiwa yakauzwa! Hali hii ilikuwa mbaya zaidi ya njaa ya wakati wa Ahabu. Ikawa mfalme alipokuwa akipita ukutani, mwanamke mmoja alimlilia mfalme awe mwamuzi au jaji wao. Mfalme akamwuliza amsaidiaje? Naye akajibu, "Mwanamke huyu aliniambia, Mtoe mtoto wako, tumle leo, na mtoto wangu tutamla kesho." Haikuwa njaa ya kawaida. Yule mama akasema walifanya vile kwa kumla mtoto wake, ila yule mwanamke mwingine hakutunza ahadi yake, "Amemficha mtoto wake." Mfalme aliposikia vile, alijua mambo ni mabaya mno, na aliyararua mavazi yake juu ukutani, maana kuta za siku zile zilikuwa pia njia pana za kutembea na magari ya farasi. Watu wakamwona mfalme amevaa magunia.

Mfalme akamlaumu Elisha, japo hii ilikuwa ni adhabu ya uovu wa mfalme na watu wake kwa kuabudu miungu mingine. Akiwa amekasirika akasema, "Mungu anifanyie hivyo, na kuzidi, kikimbakia kichwa Elisha mwana wa Shafati juu yake leo." Elisha

alikua akikaa nyumbani mwake, na wazee wakikaa pamoja naye. Mfalme akamtuma makamu wake aende kwa Elisha, ila hata kabla ya kufika, Elisha alioneshwa na kuwaambia wale wazee waliokuwa pamoja naye, akasema, “Je! mwaona jinsi huyu mwana wa mwuaji alivyotuma aniondolee kichwa changu?” Akawaambia wale wazee kuwa yule aliyetumwa akifika, wafunge mlango ili kumzuia. Yule aliyetumwa akasema, “Angalia mabaya haya yatoka kwa BWANA; kwani mimi kumngojea BWANA tena?”

Elisha akasema, “Lisikieni Neno la BWANA; BWANA asema hivi, kesho panapo saa hii, kipimo cha unga mzuri kitauzwa kwa shekeli, na vipimo viwili vya shayiri kwa shekeli, langoni pa Samaria.” Basi yule akida ambaye mfalme alikuwa akitegemea mkono wake kwa utumishi akamjibu yule mtu wa Mungu Elisha akisema, “Tazama, kama BWANA angefanya madirisha mbinguni, je! jambo hili lingewezekana? Akamwambia, Angalia, wewe utaliona kwa macho yako, lakini hutakula.” Ikawa ni kwa hasara yake kukosa imani, au kutosikia maneno ya mtu wa Mungu.

Basi walikuwapo watu wanne wenye ukoma, penye lango la mji, wakasemezana, mbona tunakaa hapa hata tufe? Tukisema tutaingia mjini, mjini mna njaa, hivyo tutakufa; na tukikaa hapa tutakuwa na njaa, pia tutakufa. Wakajipa moyo wakisema Haya! twende tukaliendee jeshi la Washami, wakituhifadhi hai tutaishi; wakituua tutakufa tu. Basi wakaondoka kabla ya mapambazuko, ili waende mpaka kituo cha Washami, na walipofika mwanzo wa kimo cha Washami, kumbe hapana mtu. Washami wote wamekimbia, kwani BWANA alikuwa amewafanya Washami kusikia vishindo vya magari na farasi, kama jeshi kubwa lililokuwa linataka kuwashambulia. Washami wakasemezana, wakifikiri mfalme wa Israeli amekodi askari wa wafalme wa Wahiti, na wa Wamisri waje wapigane nao. Washami waliondoka kukiwa giza bado wakakimbia, wakaziacha hema, farasi, na punda wao wapate kujiponya nafsi zao.

Basi wale wenye ukoma walipofika, waliingia hema moja wakala na kunywa, wakachukua fedha, dhahabu na mavazi. Wakaenda wakaficha nyara zao, wakarudi tena hema jingine, wakafanya vile vile kama hema la kwanza. Ndipo wakasemezana, “Mambo haya tufanyayo si mema, leo ni siku ya habari njema nasi tunanyamaza,” huku watu wanateseka na kula hata watoto wao!! Mioyo yao ikawachoma mpaka wakaona wasipowaambia watu wengine wenye njaa kabla hakujapambazuka, basi madhara yatawapata. Basi wakatoka waambie nyumba ya mfalme. Mfalme alikuwa amelala na alipoamka mambo yalikuwa yamebadilika. Basi wakaita walinzi wa mji na kuwaambia, “Angalia tulifika kituo cha Washami, na tazama hamna mtu yeyote huko wala sauti ya mtu, ila farasi, na punda wamefungwa kwenye mahema kama walivyoziacha. Walinzi wale wakaenda kuwaambia wa nyumba ya mfalme. Mfalme akaondoka usiku na kuwaambia watumishi wake. Lakini alifikiri kwamba Washami wanafanya hila, labda wameondoka kidogo wakingoja Waisraeli waje, kisha wawashambulie. Basi mtumishi mmoja wa mfalme akasema, kumradhi, tutwae farasi watano kati ya hao waliosalia, na kwenda kupeleleza kuhusu Washami, kama wapo karibu na wanataka kuvizia. Basi walitwaa magari mawili, na farasi zake, na kuwafuata Washami, kuangalia kama mambo ni shwari au wanataka kuwavamia. Wakawafuata mpaka Yordani, na kumbe njia yote ilikuwa imejaa

mavazi na vyombo walivyotupa Washami wapate kukimbia upesi. Basi wale waliotumwa walirudi, wakampa mfalme ripoti. Watu wakatoka kuteka nyara kwenye hema za Washami, ikawa vitu vikawa vingi, na kipimo cha unga mzuri kikauzwa kwa shekeli, na vipimo viwili vya shayiri kwa shekeli, sawasawa na Neno la BWANA.

Mfalme akamweka yule akida aliyekosa imani kwa mtumishi wa Mungu Elisha, ili asimamie watu mlangoni; lakini wingi wa watu walipopita kwa nguvu kwenda kutafuta chakula, walimkanyaga langoni akafa. Ikawa kama alivyosema mtumishi wa Mungu alipomshukia, kwamba, vipimo viwili vya shayiri kwa shekeli na kipimo cha unga mzuri kwa shekeli, ndivyo itakavyokuwa kesho, panapo saa hii, katika lango la Samaria, ila wewe utaona kwa macho yako, lakini hutakula. Tujifunze kutii sauti ya Mungu kupitia kwa watumishi Wake.

*Hakuna kitu kinachoweza kuwa kisicho cha msaada na kisichoweza kushindwa zaidi kuliko roho inayohisi kutokuwa na kitu (utupu wake), na hivyo kuzitegemea kabisa sifa za Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka (kujidondosha kabisa kwa Mwokozi). MUNGU atatuma kila malaika mbinguni kumsaidia yule anayeweka tegemeo lake lote kwa Kristo, badala ya kumruhusu kushindwa.


---

Washami walifanya jambo gani kwa Israeli? Elisha alimwahidi nini mfalme? Je, yule ambaye hakumwamini nabii alipatwa na nini? Je, kuna umuhimu gani kuamini manabii wa Mungu?

**SIKU YA 135**
**(Mei 14)**

# Hazaeli Awa Mfalme wa Shamu

**- 2 Wafalme 8**



Baada ya muda kupita, yule mwanamke Mshunami, ambaye sasa alikuwa ni mjane aliondoka nchini kwao na kwenda kuishi ugenini kwa sababu ya njaa itakayokuja. Njaa hii ilikuwa ya miaka saba. Basi yule mwanamke aliondoka, kama mtu wa Mungu alivyomwagiza, akenda kukaa katika nchi ya Wafilisti kwa miaka saba. Ikawa miaka saba ilipokwisha alirudi Israeli, akaenda kwa mfalme ili amlilie kwa ajili ya nyumba na shamba lake lililokuwa limechukuliwa. Mfalme alikuwa anazungumza na Gehazi, aliyewahi kuwa mtumishi wa Elisha, mtu wa Mungu, akamsihi, "niambie nakusihi, mambo makuu yote aliyofanya Elisha." Ikawa alipokuwa akimsimulia mfalme jinsi Elisha alivyomfufua mtu aliyekuwa amekufa, na tazama yule mwanamke Mshunami akaingia. Mwanamke huyu akamlilia mfalme kwa ajili ya nyumba na shamba lake, na Gehazi akasema, "Bwana wangu mfalme, huyu ndiye mwanamke, na huyu ndiye mwanawe ambaye Elisha alimfufua." Mfalme alipomwuliza huyu mwanamke, naye alimweleza yale ambayo alifanyiwa na Elisha. Basi ikawa ni baraka, maana mfalme alikuwa na ushahidi wa kutosha, na ndiye alikuwa na shauku ya kujua mambo ya mtumishi wa Mungu Elisha. Mfalme akamtoa mtumishi wake ashugulikiaye mambo ya uongozi, aende na huyu mama na ahakikishe amerudishiwa yote aliyokuwa nayo, na mapato yote ya shamba lake, tangu siku ile aliposafiri hata wakati ule.

Kisha Elisha aliondoka kwenda Dameski kwa Ben-hadadi, mfalme wa Shamu ambaye alikuwa mgonjwa. Naye mfalme aliambiwa ya kwamba “yule mtu wa Mungu amefika hapa.” Mfalme akamwambia mtumishi wake Hazaeli, chukua zawadi mkononi mwako uende kumlaki huyu mtu wa Mungu Elisha na umwulize “Je! nitapona ugonjwa huu.” Hazaeli alienda kumlaki akichukua zawadi mkononi mwake za kila kitu chema kinachopatikana Dameski, kiasi cha mizigo ya ngamia arobaini. Akasimama mbele ya Elisha akasema, Mwana wako, Ben-hadadi wa Shamu amenituma kwako, akitaka kujua kwamba huu ugonjwa wake atapona?” Elisha akajibu, mwambie bila shaka atapona, lakini BWANA amenionyesha ya kwamba bila shaka atakufa. Kisha Elisha alimkazia macho Hazaeli hata akatahayari, na yule mtu wa Mungu akalia machozi. Hazaeli akashangaa, kwamba Elisha analilia nini? Naye Elisha akajibu, kwa sababu nayajua mabaya utakayowatenda wana wa Israeli; utazichoma moto ngome zao, utawaua vijana wao kwa upanga, utawaua watoto wachanga na wanawake wenye mimba utawapasua. Hazaeli akashangaa na kusema lakini mimi mtumwa wako ni nani, mimi niliye mbwa tu, hata nifanye jambo hili kubwa? Elisha akamwambia, BWANA amemwonyesha kwamba yeye ndiye atakuwa mfalme wa Shamu. Hazaeli akamwacha Elisha na kurudi, kwa bwana wake. Ben-hadadi akamwuliza mambo yamekwendaje na Elisha? Akasema, bila shaka utapona. Ikawa siku ya pili yake Hazaeli akatwaa shuka, na kuichovya katika maji, akalitandaza juu ya uso wake Ben-hadadi hata akafa na Hazaeli akatawala badala yake.

Katika mwaka wa tano wa Yoramu mwana wa Ahabu mfalme wa Israeli, Yehoshafati akiwa mfalme wa Yuda, Yehoramu mwana wa Yehoshafati alianza kutawala Yuda. Alikuwa na miaka 32 na akaiendea njia ya wafalme wa Israeli, japo baba yake alimpenda Mungu. Hii ni kwa sababu alikuwa amemwoa binti wa Ahabu na Yezebeli. Hili ni kosa kubwa kwa mtu wa Mungu kufunga pingu za maisha na mtu asiyeamini. Basi huyu mfalme akafanya maovu machoni pa BWANA, ila BWANA hakutaka kuiharibu nyumba ya Yuda kwa ajili ya agano lake na Daudi.

Basi Edomu wakaasi mikononi mwa Yuda, na kujifanyia ufalme wao. Yehoramu akaenda mpaka Sairi na magari yake yote pamoja naye. Alitoka usiku, akawapiga Waedomi waliomzunguka, na maakida wa magari na watu wakakimbilia hemani mwao.

Yehoramu akafariki na mwanawe akatawala, mwaka wa kumi na mbili wa Yoramu mfalme wa Israeli. Ahazia alianza kutawala na miaka 22 na jina la mamaye lilikuwa Athalia, binti wa Ahabu na Yezebeli. Ahazia aliendea njia za Ahabu babu yake na Yezebeli bibi yake. Basi tunaambiwa hakufuata njia za babu yake mzaa baba, yaani, Yehoshafati, bali babu mzaa mama. Uovu ni kama nguvu ya uvutano, yaani kwenda chini ni rahisi kuliko kwenda juu, ni neema ya Mungu kwamba hatuangamii na anatusaidia tupande juu tena. Ahazia akaenda pamoja na Yoramu kupigana na jeshi la Washami na mfalme wao Hazaeli kule Ramoth-gileadi nao wakamtia majeraha. Basi Ahazia akaenda kumtazama Yoramu aliyekuwa mgonjwa.

Elisha alikuwa mzee sasa na akamtuma mwana wa manabii aende kumpaka mafuta Yehu kuwa mfalme wa Israeli kule Ramoth-gileadi. Basi mtumishi alienda

na kumtoa kati ya ndugu zake, kisha akampeleka chumba cha ndani, na kumpaka mafuta, kisha akakimbia kwa haraka.

*Wale Wanaotafuta Msamaha Lazima Wenyewe Wawe na Tabia ya Kusamehe—Tunapokuja kuomba rehema na baraka kutoka kwa MUNGU tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha katika mioyo yetu wenyewe. Tunawezaje kuomba basi, "Utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu," na bado tuwe na roho ya kutosamehe? Mathayo 6:12. Ikiwa tunatazamia sala zetu kusikiwa ni lazima tuwasamehe wengine kwa namna ile ile na kwa kiwango kile kile tunachotamani kusamehewa.

---

Elisha alimwambia mwanamke wa Shunemu kufanya nini? Gehazi alimwambia nini mfalme? Yehu alipakwa mafuta na nani? Mama ya Ahazia aliitwa nani? Kwa nini ni vigumu kufuata wazazi wetu wazuri, na rahisi kufuata wazazi wetu waovu? Kisa hiki kinatupatia fundisho gani?

**SIKU YA 136**
**(Mei 15)**

# Utawala wa Yehu

**- 2 Wafalme 9-10**



Yehu akapewa maagizo ya BWANA kupitia kwa nabii Elisha aliyemtuma mmoja wa wana wa manabii, jinsi alivyopaswa kuitendea nyumba ya Ahabu bwana wake, ili BWANA ajilipize kisasi cha damu ya watumishi Wake manabii na damu ya watumishi wote wa BWANA mikononi mwa Yezebeli. BWANA akasema nyumba yote ya Ahabu itaangamia, watoto wote wa kiume watakatika. Na nyumba ya Ahabu itakuwa kama nyumba ya Yeroboamu na Baasha, walioabudu miungu mingine na kupata adhabu. Mjumbe alimuita Yehu chumbani na akamtia mafuta awe mfalme wa Israeli na kumpatia ujumbe. Walipotoka ndani, wenzake wakamwuliza Yehu, mwana wa nabii alitaka nini kwako au ni mwenda wazimu? Naye akasema kwa kupoteza lengo "ninyi mnamjua mtu huyu na habari ya maneno yake." Wakamwambia amekwambia nini? Naye akawaambia, amenitawaza kuwa mfalme wa Israeli, na kuniambia niiharibu nyumba ya Ahabu. Basi watu hawa, wakafanya haraka kutangaza, "Yehu ni mfalme," hivyo Yehu akawa mfalme, na kufanya kama alivyoagizwa. Wakati huo Yoramu alikuwa akiulinda Ramoth-gileadi kwa sababu ya Hazaeli mfalme wa Shamu, naye alikuwa amerudi apate kupona jeraha zake

alizotiwa na Washami. Yehu akapiga mbio na gari lake la farasi kwa kasi kama alivyojulikana kuendesha.

Basi, mlinzi alikuwa amesimama juu ya mnara wa Yezreeli, aliliona kundi la watu wa Yehu, alipokuwa akija, akasema, naona kundi la watu. Yoramu akaagiza mtu atumwe kwenda kuwalaki na kuuliza, "je, ni amani?" Basi mpanda farasi mmoja akaenda ili kuwalaki na kuuliza, Je! Ni amani? Yehu akajibu kwa jeuri, "wewe una nini na amani, geuka unifuate."Yule mlinzi akatoa taarifa kuwa mjumbe amewafikia ila harudi. Wakatuma mpanda farasi wa pili, naye alipowafikia akasema, mfalme auliza, "Je ni amani?" Yehu akasema mara ya pili, "wewe una nini na amani, geuka unifuate." Yule mlinzi akatoa habari tena, amewafikia wala harudi tena, na mwendo huu ni kama mwendo wa Yehu mwana wa Nimshi, maana analiendesha gari kwa kasi. Yoramu akasema, tandika gari, wakalitandika gari lake naye akaenda na Ahazia shemeji yake mfalme wa Yuda, kila mtu kwenye gari lake, wakamkuta Yehu kwenye kiwanja cha Nabothi. Yoramu alipomwona Yehu alisema, "Je! ni amani Yehu? Akajibu, Amani gani, maadamu uzinzi wa mama yako Yezebeli na uchawi wake ni mwingi. Yoramu akageuza mikono yake akakimbia, akimwambia Ahazia, ni uhaini, Ahazia." Yehu akavuta upinde wake kwa nguvu akampiga Yoramu hata mshale ukamtoka penye moyo wake, naye akaanguka katika gari lake, akafa. Ndipo Yehu akamwambia akida wake aende akamtupe kwenye kiwanja cha Nabothi. Neno la BWANA likatimia, "Nitakulipa katika kiwanja hiki, asema BWANA." Ahazia ambaye mama yake alikuwa ni Athalia, binti Yezebeli, alikuwa mfalme wa Yuda, alipoona hayo, akakimbia na Yehu alimfuatia na akampiga akafia pale Megido.

Yehu hakuishia pale, bali alimfuata Yezebeli huko Yezreeli. Mwanamke huyo mwovu alipopata habari alitia wanja machoni, akapamba kichwa chake. Pengine alitaka apendeze. Yehu alipoingia Yezreeli, Yezebeli alisema, "Je! ni amani, Ewe Zimri mwenye kumwua bwana wako?" Yehu akaamrisha atupwe ghorofani, basi wakamtupa chini ya ukuta akafa, na farasi wakamkanyaga. Walipotaka kumzika walikuta sehemu nyingi zimeliwa na mbwa, na mzoga wake ukawa kama mavi juu ya uso wa mashamba.

Watu wakasema wako tayari kuwa chini ya Yehu. Akawaambia kama wanataka kuwa upande wake waueni wana 70 wa Ahabu ambao ni warithi. Mungu alimfadhili kwa ajili ya uovu wa Ahabu. Akawaambia manabii wote wa Baali waje, kwamba yu pamoja nao, kumbe ilikuwa ni hila. Basi wakaja watu wengi nyumbani mwa Baali, hakuna aliyebaki. Akawaambia wafanye ibada ya Baali, walipomaliza, aliwaua wote wale walioabudu Baali. BWANA akamwambia, "kwa kuwa umetenda vema kwa kufanya vilivyo haki machoni pangu… wana wako wa kizazi cha nne watakaa kitini mwa Israeli." Lakini hakuangalia sheria ya BWANA, Mungu wa Israeli, moyo wake wote hakutoka katika makosa ya Yeroboamu, ambayo kwa hayo aliwakosesha Israeli. Yehu alitawala Israeli katika Samaria miaka 28, alipokufa mwanawe Yehoahazi akatawala mahali pake.

Yehu aliwakosesha Israeli kwa kuabudu zile ndama za dhahabu zilizokuwapo Betheli na Dani. Pengine tunashangaa hawa wafalme na watu wa zamani walivyoabudu sanamu, lakini hata siku hizi, kuna watu wanaabudu miungu mingine, iwe ni sanamu,

michezo, chakula, runinga, kompyuta, maoni, urembo, marafiki, mitindo, elimu ya uongo na mingineyo. Nilichukua masomo ya elimu ya viumbe kama shahada na nikasoma pia uibukaji. Cha ajabu, elimu kale (elimu ya mambo ya kale) inaafikiana na miaka ya Neno la Mungu! Kwa neema ya Mungu, hebu tusiwe miongoni mwa watu wanaoabudu sanamu au kuwa na miungu mingine. Mungu wetu awe ni BWANA wa maisha yetu, Yeye tu, peke yake.

*Baada ya kumaliza Sala ya Bwana, Yesu aliongeza hivi: "Mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi; bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu. Mathayo 6:14, 15. Yeye asiyesamehe anafunga/anafunga kila mfereji ambao kwa huo peke yake anaweza kupokea rehema kutoka kwa MUNGU. Hatupaswi kufikiri kwamba wale waliotuumiza wasipokiri kosa lao, sisi tuna haki ya kuwanyima msamaha wetu. Ni sehemu ya wajibu wao, bila shaka, kunyenyekeza mioyo yao kwa toba na maungamo; lakini tunapaswa kuwa na roho ya huruma kwa wale ambao wametukosea, haijalishi kamawameungama makosa yao kwetu au la.

---

Mazuri aliyofanya Yehu yalikuwa yapi? Mabaya ya Yehu yalikuwa yapi? Ukijua una saa chache za kuishi, je, utapaka wanja kwanza au utaungama dhambi zako ili Yesu akija uishi naye milele? Yehu alimwangamizaje Yezebeli? Nani alimwambia Yehu aangamize familia ya Ahabu?

**SIKU YA 137**
**(Mei 16)**

# Yoashi-Mfalme Mtoto

**- 2 Wafalme 11-13; 2 Mambo ya Nyakati 24**



Athalia, mama yake Ahazia, alipoona mwanawe ameuawa na Yehu, akainuka na kuwaua wazao wote wa kifalme na akatawala miaka sita. Uovu wa ajabu! Kuua wajukuu wake, au watoto wa Ahazia! Athalia alikuwa binti ya Ahabu na Yezebeli. Akaishi ile mithali isemayo, 'mtoto wa nyoka ni nyoka.' Basi, Yehosheba, binti wa mfalme Yehoramu, na dada ya Ahazia, mfalme aliyeuawa, akamtwaa Yoashi, mwana wa Ahazia miongoni mwa hao wana wa kifalme waliouawa, yeye na mlezi wake akawaficha usoni pa Athalia hivyo hawakuuawa. Mwaka wa saba, Yehoyada, kuhani mkuu, ambaye mke wake alikuwa Yehosheba binti mfalme, akatuma wakuu wa mamia na walinzi ili wamtawaze Yoashi kuwa mfalme alipokuwa na miaka 7. Akaweka watu wa kulinda usalama na ngao na mikuki iliyokuwa ya mfalme Daudi. Akamleta nje mwana wa mfalme Yoashi, akamvika taji, na kumpa ushuhuda na kumtia mafuta. Watu wakapiga makofi, na kusema mfalme aishi. Athalia aliyekuwa anatawala aliposikia sauti za walinzi na watu aliingia nyumbani mwa BWANA, akatazama na kuona mfalme Yoashi amesimama karibu na nguzo, nao wakuu wanapiga baragumu karibu na mfalme na watu wanafurahi, ndipo Athalia akararua mavazi yake, akalia ni "Fitina! Fitina!" Yehoyada kuhani akawaamuru wakuu na majemadari wamtoe katika hekalu na kumwua kwa upanga ila si nyumbani mwa BWANA.

Mfalme Yoashi akafanya mapatano kati ya BWANA na mfalme na watu, ili wawe watu wa BWANA. Watu wakaiendea nyumba ya Baali wakaiangusha, na kuangusha madhabahu zake na sanamu zake wakazivunja-vunja. Yehoyada akaweka maakida juu ya nyumba ya BWANA. Watu wote wa nchi wakafurahi na mji ukatulia. Zekaria aliyekuwa nabii alikuwa mtoto wa kuhani huyu Yehoyada, na alikua pamoja na Yoashi kama wanandugu. Yoashi alisaidiwa na kuhani kutawala kwani alikuwa bado mdogo. Yoashi alitawala miaka 40; alijitahidi kufanya mema machoni pa BWANA siku zake zote ambazo kuhani Yehoyada alikuwa

naye akimfundisha. Hakika wazazi wanaompenda Mungu hatuwezi kuwalipa kwa mahangaiko waliyotuhangaikia toka kuzaliwa kwetu. Tunachoweza kufanya ni kuwahudumia na kuwasaidia katika shuguli au shida zao. Pengine binadamu anavyoweza kulipa masumbufu aliyowapa wazazi ni kwa kulea watoto wake au kusaidia kulea watoto katika njia inayopasa.

Yoashi akawaambia makuhani, fedha yote ya vitu vitakatatifu iliyoletwa nyumbani mwa BWANA, waiweke na wafanyie ukarabati wa nyumba ya BWANA. Nyumba ambayo alilelewa miaka yake saba ya awali. Ilikuwa imepita miaka 200 toka kujengwa hekalu la Sulemani. Mataifa kama Misri, Wafilisti na hata malkia Athalia walikuwa wamevunja nyumba hii na kuchukua vitu. Mwaka wa ishirini na tatu wa mfalme Yoashi, makuhani walikuwa bado hawajafanya ukarabati wakizembea agizo lake, naye akawauliza, "mbona hamtengenezi mabomoko ya nyumba." Akawaambia wasipokee fedha tena, mpaka wafanye matengenezo. Yehoyada kuhani akachukua kasha kubwa akatoboa tundu katika kifuniko chake na kuweka karibu na madhabahu ili watu watoe sadaka ya hiari waingiapo nyumbani mwa Bwana kama mfalme alivyoshauri. Makuhani walilinda na kuihesabu na karani wa mfalme. Bila shaka mfalme mwenyewe alitoa kitu, ili kuweka mfano mzuri. Hata leo tukienda hekaluni, ni vyema kuwa na sadaka. Ni aibu kama tuna kitu halafu tunakwenda mbele za Mungu mkuu bila kitu, bali tukienda mpirani au dukani tunakuwa na pochi zenye pesa tele. Mtu mmoja jirani yangu alisema dola moja ilipoulizwa ulikuwa wapi, ilisema kanisani, kanisani, kanisani. Mungu ni mwenye rehema maana kila siku tunafadhiliwa naye, na tunaendelea kuomba vitu tele, ila tukija kwake tunatoa vidogo vya kusaidia wengine kwa mahitaji!!

Basi haikuchukua muda kasha likajaa, dhahabu, shaba na kila vito. Walimwaga, na kuweka tena ili watu watoe sadaka. Walitafuta maseremala, waponda mawe, waashi, na wajenzi wasimamie na kufanya kazi katika nyumba ya BWANA, kazi ya kukarabati mabomoko. Pesa zilikidhi matumizi ya vifaa vyote na kulipa mafundi, na ilyobaki walinunua vyombo vya hekalu. Je, wewe leo na wazazi wako mna vitu vya kutoa sadaka bali mnaviweka ndani ya nyumba miaka na miaka? Hata mimi nimegundua nina vingi vya kutoa vimekaa miaka kadhaa, naomba Mungu anisaidie nivitafute na kuvitoa mwaka huu.

Sadaka za matoleo ya kosa na dhambi haikuletwa kukarabati nyumba ya BWANA, hiyo ilikuwa ya makuhani wenyewe. Kuhani Yehoyada aliishi miaka 130 akawa mzee, na alipokufa, wakuu wa Yuda walimwendea mfalme na kumsujudu. Mfalme akaingizwa katika uovu. Wakaiacha ibada ya kweli na wakatumikia maashera na sanamu, BWANA akapeleka manabii kuwashuhudia ila hawakukubali kusikiliza. Naye Mungu akauliza, "kwa nini ninyi kuzihalifu amri za BWANA, hata msiweze kufanikiwa?"

Kisha Hazaeli, mfalme wa Shamu alikwea Gathi na kuitwaa, kisha akaelekeza uso kuitwaa Yerusalemu, akachukua vyote walivyoviweka wakfu Yehoshafati na Yehoramu na Ahazia baba zake wafalme wa Yuda. Yoashi alibadilika akiwa mtu mzima, akafanya yaliyo mabaya machoni pa BWANA, hata Zekaria nabii, na mwana wa kuhani Yehoyada alitumwa kumwambia, "kwa nini ninyi kuihalifu amri

za Bwana? kwa kuwa mmemwacha BWANA, yeye naye amewaacha ninyi." Badala ya kusikia maneno ya mausia ya binamu yake na kaka yake, wakafanya shauri juu yake huyu nabii, wakampiga kwa mawe kwa amri ya mfalme katika ua wa nyumba ya BWANA. Akasahau fadhila za kuhani yule na mkewe kulinda maisha yake alipokuwa mdogo, wakati bibi yake Athalia alipotaka kumwua. Hakuukumbuka tena wema wake, alifanya mema wakati baba ya Zekaria akiwa hai, na sasa alimwua mwanawe. Naye nabii Zekaria alipokufa alisema "BWANA na ayaangalie haya, akayatakie kisasi." Jeshi la Washami lilikuja, na lilimfadhaisha Yoashi, mpaka akashikwa sana na maradhi; watumishi wake wakamfanyia fitina kwa ajili ya damu ya Zekaria, wakamwua kitandani pake, akafa. Tuombe hili lisitokee kwetu, kuanza vizuri, na kuishia vibaya kwa sababu ya marafiki waovu.

Basi, mwanawe Amazia alitawala mahali pake. Huyu alikuwa mwovu, na Israeli walikuja na kubomoa sehemu ya ukuta wa Yerusalemu, na kuchukua dhahabu yote na fedha, na vyombo vyote vilivyoonekana katika nyumba ya BWANA na katika hazina ya nyumba ya mfalme, na watu kuwa amana.

Katika mwaka wa 23 wa mfalme Yoashi mwana wa Ahazia, Yehoahazi mwana wa Yehu alianza kutawala juu ya Israeli na Samaria, kwa miaka 17. Akafanya maovu machoni mwa BWANA. BWANA akawatia mikononi mwa mfalme wa Shamu, kwa Hazaeli na Ben-hadadi. Yehoahazi akamsihi BWANA naye akamsikiliza, na kuwapa mwokozi, nao wakatoka mikono mwa Washami; nao wakakaa hemani mwao kama zamani. Lakini hawakuyaacha makosa ya nyumba ya Yeroboamu, ambaye aliwakosesha Israeli kwa ashera, iliyokaa Samaria.

Yehoahazi akafa na mwana wake Yehoashi akatawala mahali pake, katika mwaka wa 37 wa Yoashi mfalme wa Yuda. Yehoashi alitawala miaka 16, akafanya yaliyo maovu machoni pa BWANA. Yehoashi alifariki na kulala na babaze na Yeroboamu akakaa katika kiti chake cha enzi. Yeroboamu, hili jina limerudiwa, ni kama lile la mfalme wa kwanza wa Israeli ilipogawanyika.

Elisha alikuwa ameshikwa na ugonjwa uliomwua. Sasa alikuwa mzee na alikuwa amemtumikia BWANA akizungumza na wafalme, manabii na watu wa kawaida. Wengine walimpenda na wengine walimchukia. Ndivyo hata leo watumishi wa Mungu wanavyochukuliwa. Alikuwa si mtumishi wa mshahara, kwani ni Mungu mwenyewe alimlipa. Wakati wa shida na njaa alikuwa kimbilio kwa wengi. Basi akiwa kitandani ameshikwa na ugonjwa, Yehoashi mfalme wa Israeli akashuka kwake amtazame. Akamlilia akisema, "Baba yangu! Baba yangu! Gari la Israeli na wapanda farasi wake!" Maneno haya yalikuwa ya heshima, yakionesha kumthamini nabii huyu kama baba wa taifa, na hasa wakati huu alipopoteza magari yake ya farasi kwa mfalme wa Shamu. Elisha akamwambia atwae uta na mishale. Elisha akaweka mikono yake juu ya mikono ya mfalme. Akamwambia afungue dirisha lililoelekea mashariki, na kupiga. Alipopiga mshale, Elisha alimwambia "mshale wa BWANA wa kushinda, naam, mshale wa kushinda Shamu, kwa maana utawapiga Washami katika Afeki hata utakapowaangamiza." Akamwambia mfalme wa Israeli tena, piga chini mishale. Naye akapiga mara tatu kisha akaacha. Mtu wa Mungu Elisha akakasirika, akasema "ingalikupasa kupiga mara tano au mara sita, ndipo

ungaliipiga Shamu hata kuiangamiza; bali sasa utaipiga Shamu mara tatu tu. Elisha akafa, nao wakamzika.

Basi vikosi vya Wamoabi wakaingia katika nchi mwanzo wa mwaka. Ikawa walipokuwa wakimzika mtu, angalia waliona kikosi; wakamtupa yule mtu kaburini mwa Elisha; mara yule maiti alipoigusa mifupa ya Elisha, alifufuka, akasimama kwa miguu. Mifupa ya mtu wa Mungu ikatenda mwujiza. Hata katika kifo chake, alikuwa akitimiza utume wa Mungu. Hata leo nasi, kuna mengi mema yataendelea kufanyika hata tutakapolala usingizi wa mauti, kama tumewekeza kwa Bwana!

*Katika sala ambayo Kristo aliwafundisha wanafunzi Wake kulikuwa na ombi: Utusamehe makosa yetu kama sisi tunavyowasamehe wanaotukosea. Hatuwezi kurudia sala hii kutoka moyoni na kuthubutu kuwa watu tusiosamehe, kwani tunamwomba Bwana atusamehe makosa yetu dhidi Yake kama vile sisi tunavyowasamehe wanaotukosea. Lakini ni wachache wanaotambua umuhimu wa kweli wa sala hii. Ikiwa wale wasiosamehe wangeelewa kina cha maana yake wasingethubutu kuirudia hii sana na kumwomba MUNGU awashughulikie kama wanavyoshughulika na wanadamu wenzao wafao.

---

Athalia alifanya uovu gani? Yoashi alifichwaje? Mwana wa Yehu alikuwa mfalme wa aina gani? Yule maiti alifufuka alipogusana na kitu gani? Wakati wa Yoashi ufalme ulikuwa ukoje?

**SIKU YA 138**
**(Mei 17)**

# Kwaya Iliyoshinda Vita

**- 2 Wafalme 19-20**

Si mara nyingi tunasikia kwaya ikiongoza jeshi la nchi, bali hili litokea wakati Yehoshafati akiwa mfalme wa Yuda. Siku moja alikuja mjumbe na kusema kwamba Wamoabi, Waamoni na Wameuni wako njiani na maelfu ya wanajeshi kuja kuvamia mji na wako En-gedi. Mfalme Yehoshafati akijua kwamba jeshi lake ni dhaifu, akaogopa, akauelekeza uso wake amtafute BWANA na kuomba msaada. Alikuwa amefanya makosa huko nyuma kwa kushika urafiki na Ahabu, ila aliungama, Basi Akatangaza mbiu ya kufunga na kuomba. Akisema Watu wote waje kwenye nyumbani mwa BWANA ili kuomba. Wakaja watu wengi, wanaume, wanawake, watoto, wakitoka pande zote. Lilikuwa jambo la peke yake kwani lilionesha unyenyekevu kwamba "msaada wetu watoka kwa BWANA" na si ukubwa wa jeshi, ujanja wa vita, au teknolojia na silaha nyingi. Yehoshafati akaleta kusanyiko nyumbani mwa BWANA mbele ya ua mpya. Yehoshafati akampa Mungu sifa na utukufu. Katika maombi yetu hili ni muhimu, tunampatia Mungu sifa na utukufu, kwa kuzungumzia tabia yake na matendo yake makuu. Yehoshafati akasema, Mungu wa baba zetu, Ndiye atawalaye falme zote za mataifa, "mkononi mwako mna uweza na nguvu, asiweze mtu yeyote kusimama kinyume chako. Si wewe, Ee Mungu wetu, uliyewafukuza wenyeji wa nchi hii mbele ya watu wako Israeli, ukawapa wazao wa Ibrahimu, rafiki yako, hata milele?" Akaendelea kusema kwamba Waisraeli walijenga patakatifu kwa Jina lake, wakisema, "yakitujia mabaya, upanga, hukumu, tauni, njaa, tutasimama mbele ya nyumba hii na mbele zako, maana jina lako limo katika nyumba hii." Akasema, wakilia katika shida zao, BWANA atasikia na kuokoa. Akamweleza BWANA kuwa sasa wana wa Moabu, Amoni na wa milima ya Seiri ambao hukuwaacha Israeli kuingia katika nchi yao wakati walipotoka Misri; tazama jinsi wanavyotulipa, wakija kututupa toka milki yako, uliyoturithisha. Akauliza kama BWANA atawahukumu, akasema, "macho yetu yatazama kwako, maana sisi hatuna uwezo juu ya jamii kubwa hii, wanaotujia juu yetu, wala hatujui tufanyeje, lakini macho yetu yatazama kwako." Ndipo Yahazieli mwana wa Zekaria, Mlawi, akajiliwa na roho ya BWANA na kutabiri hivi, "Msiogope wala msifadhaike kwa ajili ya jeshi kubwa hili; kwani vita si yenu bali ni ya Mungu." Akawaambia kesho yake washuke juu yao, na wangewapata penye mwisho wa bonde. Akawaambia hawahitaji kupigana, bali wajipange na wakauone wokovu wa Bwana ulio pamoja nao. Mfalme Yehoshafati akaanguka kifudifudi mbele za BWANA na wote wakaao Yerusalemu, wakamsujudia BWANA, ikasimama kwaya ya Walawi, Wakohathi na wana wa Wakorahi wakiimba kwa sauti kuu wakimsifu Mungu.

Wakaamka asubuhi na mapema, wakaenda katika jangwa la Tekoa, na walipokuwa wakitoka Yehoshafati kwa ujasiri alizungumza na watu akisema, "Nisikieni wenyeji wa Yuda, na Yerusalemu; "Mwaminini BWANA, Mungu wenu, ndivyo mtakavyothibitika, waaminini manabii wake, ndivyo mtakavyofanikiwa." Kila mtu



aliafiki, wakijua kuwa watashinda. Mfalme akafanya mipango ya kushauriana na watu. Akaweka wale watakaomwimbia BWANA na kumsifu katika uzuri wa utakatifu, wakaenda mbele ya jeshi na kuimba wakisema, "Mshukuruni BWANA; kwa maana fadhili Zake ni za milele." Walipoanza kuimba na kusifu, BWANA akaweka waviziao juu ya wana wa Amoni, Moabu na Seiri nao wakapigwa vibaya. Walipigana wao kwa wao, yaani, wana wa Amoni na Moabu wakawaua na kuwaharibu wale wa mlima wa Seiri, kisha wakageukiana wao wenyewe. Wana wa Yuda walipofika mnara wa kulindia jangwani waliona maiti walioanguka chini, wala hapana aliyeokoka.

Mfalme Yehoshafati na watu wake walichukua nyara za vitu vyao. Wakaona adui alikuwa na mali nyingi, kama vile mavazi, vito, johari, nk. Zilikuwa nyingi zaidi ya wawezavyo kuchukua, na iliwachukua siku tatu kuchukua nyara hizi maana zilikuwa nyingi sana. Siku ya nne wakakusanyika katika bonde la Baraka, na kulibariki jina la BWANA, wakamsifu na kutoa shukurani. Bonde hilo likaitwa bonde la Baraka. Wakarudi kwao na mfalme wao Yehoshafati ametangulia, kwa furaha kwa kuwa BWANA alikuwa amewafurahisha kwa kuwashugulikia adui zao.

Wakafika Yerusalemu wenye vinanda, vinubi na mapanda kwenda nyumbani mwa BWANA hekaluni. Falme za jirani zikapata hofu, kwa kuwa walisikia BWANA amewapigania adui zao. Basi ukatulia ufalme wake Yehoshafati, kwa sababu Mungu wake alimstarehesha pande zote. Hakuna jambo linalopendeza kama kumsifu BWANA kwa nyimbo, nyimbo mpya na hata za zamani, "Msemezane kwa zaburi, na tenzi, na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia BWANA mioyoni mwenu. Na kumshukuru Mungu Baba siku zote, kwa mambo yote, katika jina lake BWANA wetu Yesu Kristo. Hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo."

Kama binadamu, mara zingine tunatetereka. Maana mwana wake Yehoshafati akamwoa Athalia binti wa Ahabu na Yezebeli. Kutaka kupendeza upande wa wakwe zake, mfalme Yehoshafati alifanya jambo baya baadaye kujiunga na mfalme Ahazia kufanya biashara Tarshishi kwa merikebu. BWANA alimtuma Eliezeri nabii,

akisema “Kwa sababu umepatana na Ahazia, BWANA amezivunja vunja kazi zako.” Ndipo zikavunjika merikebu, zisiweze kufika Tarshishi. Hata leo tuwe waangalifu tunapochagua marafiki, au wenzi wa maisha, tusifungiwe nira na wale wasioamini, maana watatupeleka nje ya mapenzi ya Mungu, nasi tutajikuta tunataka kuwapendeza hata kwa yale ambayo ni maovu. Hatuwezi kutumikia mabwana wawili, Mungu na Shetani, lazima tuchague mfalme moja tu.

Muziki unaweza kuwa nguvu kubwa kwa wema ukitumiwa vyema katika ibada. Muziki pia unasaidia kufundisha Maandiko. Ni mara chache tunasahau yale ambayo tumeimba toka tukiwa wadogo. Uimbaji usifanywe kwa msukumo au mihemko. Muziki unapaswa kuwa na uzuri, kanuni na nguvu. Acha sauti zipande juu kwa nyimbo za sifa na ibada nazo zitakuwa sadaka inayokubalika mbele za Mungu. Kuimba, ni sehemu ya huduma ya kidini, ni tendo la ibada kama vile sala. Hebu tunapokuwa kanisani, wimbo unapoendelea tuimbe pamoja na wengine. Vijana wengi huwa hawaimbi wakati waumini wanapoendelea kumwabudu Mungu kwa nyimbo.

*Tunahitaji kuchunguza mioyo yetu kama matayarisho ya kwenda mbele za MUNGU katika maombi, ili tujue sisi ni wa roho ya namna gani. Ikiwa hatutawasamehe wale waliotukosea, maombi yetu ya msamaha hayatasikilizwa. “Utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu.” Sisi kama wadhambi tunapokaribia Kiti cha Rehema, hatuwezi kueleza hisia ya ombi hili bila msamaha mioyoni mwetu kwa wale wote ambao wametuumiza. Juu ya ombi hili Yesu anatoa maelezo: “Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi; bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.”

---

Ni mataifa gani yaliungana ili kuipiga Yuda? Kwa nini kwaya iliimba? Kwa nini ni muhimu kumtegemea BWANA? Kosa gani alilofanya mfalme Yehoshafati? Kwa nini ni vyema kukumbuka kumshukuru Mungu akitusaidia? Unaweza ukatoa faida tano za kuimba au nyimbo kwa mwili wa binadamu?

**SIKU YA 139**
**(Mei 18)**

# Miaka ya Uovu wa Wafalme

**- 2 Wafalme 14-15 na 2 Mambo ya Nyakati 25- 28**




Hazaeli, mfalme wa Shamu akawaonea Waisraeli siku za Yehoahazi, lakini BWANA akawahurumia, akawasikitikia na kuwaangalia kwa ajili ya agano lake na Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Wala hakutaka kuwaangamiza au kuwatupa usoni pake bado. Alipokufa Hazaeli, alitawala Ben-hadadi mwanawe, na Yehoashi mwana wa Yehoahazi akaitwaa tena mkononi mwa Ben-hadadi miji ile aliyoitwaa yeye mkononi mwa Yehoahazi baba yake vitani. Mara tatu Yehoashi akamshinda akairudisha miji ya Israeli.

Katika mwaka wa pili wa Yehoashi, mwana wa Yehoahazi mfalme wa Israeli Amazia mwana wa Yoashi mfalme wa Yuda alianza kutawala. Alikuwa na miaka 25 alipoanza kutawala, na akatawala miaka 29 katika Yerusalemu, naye akafanya yaliyo mema machoni pa BWANA ila si kama Daudi. Alifanya kama Yoashi babaye ila hakuondoa mahali pa juu, watu wakaendelea kutoa dhabihu na kufukiza uvumba katika mahali pa juu. Ufalme ulipokuwa imara aliwaua watumishi wale waliomuua baba yake mfalme. Ila hakuua watoto wa wauaji, kwa vile BWANA aliamuru watoto wasife

kwa kosa la baba au baba asife kwa makosa ya watoto, lakini kila mtu atakufa kwa kosa lake mwenyewe. Akawaua Waedomi katika bonde la chini, akafanya kosa la kuleta miungu yao na kuisimamisha na kuisujudia akifukiza uvumba. BWANA akamtuma nabii kumwambia, "mbona umetafuta miungu ya watu isiyowaokoa watu wao mkononi mwako?" Mfalme akamjibu nabii kwa jeuri, "Je! tumekuita wewe kuwa mshauri wa mfalme? Nyamaza, kwa nini upigwe?" Nabii akaacha kusema akijua mfalme ataangamizwa kwa kutosikia sauti ya BWANA.

Amazia alituma ujumbe kwa Yehoashi mwana wa Yehoahazi, mwana wa Yehu mfalme mwa Israeli akasema "njoo tuonane uso kwa uso." Naye Yehoashi mfalme wa Israeli akatuma kwa Amazia mfalme wa Yuda maneno akisema, "Mbaruti uliokuwako Lebanoni ulituma ujumbe kwa mwerezi uliokuwa Lebanoni kusema, 'umwoze mwanangu binti yako, kukapita hayawani aliyekuwawako Lebanoni, akaukanyaga ule mbaruti. Kweli umepiga Edomu, na moyo wako umetukuka ujisifu basi, ukae nyumbani mwako. Mbona unataka kujitia bure katika madhara, hata uanguke wewe na Yuda pamoja nawe. Lakini Amazia hakutaka kusikia, basi Yehoashi mfalme wa Israeli akakwea, wakatazamana uso kwa uso na Amazia mfalme wa Yuda huko Beth- shemeshi ulio Yuda. Yuda wakashindwa mbele ya Israeli, wakakimbia kila mtu hemani mwake. Yehoashi mfalme wa Israeli akamtwaa Amazia mfalme wa Yuda na mwanawe Yoashi mwana wa Ahazia huko, akaja Yerusalemu na kuuvunja ukuta wa Yerusalemu toka lango la Efraimu hata lango la pembeni. Akaitwaa dhahabu na fedha na vyombo vilivyoonekana katika nyumba ya Mungu, na nyumba ya mfalme. Akatwaa na watu kuwa amana, akarudi Samaria. Basi mambo yote ya Yehoashi aliyofanya yameandikwa katika kitabu cha tarehe cha wafalme wa Israeli. Yoashi akalala na baba zake akazikwa Samaria na Yeroboamu mwanawe akatawala.

Katika 2 Mambo ya Nyakati 2:2, 9 tunaambiwa Amazia "Alitenda yaliyo mema mbele ya Mwenyezi-Mungu ingawa hakuyatenda kwa moyo mnyofu". Kuwa na moyo nusu ni nusu ni kuwa vuuguvugu, ni kutotii kwa ufupi! Na pale Mungu alipomwambia arudishe majeshi yake ya kukodiwa, alisema ameshayalipia tayari sasa hawezi kuyarudisha! Mungu akasema atamsaidia bila hilo jeshi, naye hakutaka kuona hilo. Ni kama siku ambayo mmeamua kufunga saumu na mtu akakupa chakula fulani, ukasema sasa sitafunga leo, ila kesho mpaka nimalize hiki chakula, au mtu mzima akiamua kuchukua mke wa pili, na Mungu akamwambia amrudishe huyo mke kwao kama alivyomwambia Ibrahimu. Naye mtu huyo aseme hapana nimeshamlipia mahari tayari, nitamrudishaje kweli!

Naye Amazia mwana wa Yoashi mfalme wa Yuda akaishi baada ya kufa kwake Yehoashi mwana wa Yehoahazi mfalme wa Israeli miaka kumi na mitatu. Wakafanya fitina juu yake katika Yerusalemu, naye akakimbia mpaka Lakishi, lakini wakatumwa watu kumfuata wakamwua huko. Akaletwa na kuzikwa Yerusalemu, kisha watu wa Yuda walimtwaa Uzia, aliyekuwa na umri wa miaka 16 wakamweka awe mfalme mahali pa baba yake. Huyu akaurudisha Elathi kwa Yuda. Uzia alifuata mashauri ya nabii Zekaria alipokuwa hai, ila alipokuwa na nguvu moyo wake ulipata kiburi na akamwasi Mungu. Uzia alitawala kwa muda mrefu wa miaka 52. Aliingia hekaluni kufukiza uvumba, juu ya madhabahu, lakini Azaria kuhani aliingia nyuma yake na makuhani 80 mashujaa ili asijipe laana, kwani ni kazi takatifu ambayo

Mungu aliwapatia ukoo wa Haruni tu. Mfalme Uzia akaghadhibika, huenda aliwaza “mimi ni mfalme, ananiambia nini huyu wa chini yangu?” Palepale akiwa na chetezo mkononi, ukoma ukamtokea kwenye paji la uso. Makuhani wakamtoa upesi, naye akatoka kwa haraka maana aligundua amepigwa kwa ukoma kama laana. Akawa na ukoma siku za maisha yake yote. Kiburi ni kitu kibaya, hata leo watumishi wa Mungu wanapotuonya, tusijifanye kwamba tunaweza kufanya shughuli yao, na tunajua mengi kwani wao ni nani? Kiburi kilimfanya mfalme Uzia aishi kwa kutengwa kwa kuwa alikuwa najisi. Hakuweza kuishi na watoto wake, au mke wake, kwani alitengwa kwa kujitakia.

Katika mwaka wa 15 wa Amazia mwana wa Yoashi mfalme wa Yuda, Yeroboamu mwana wa Yehoashi mfalme wa Israeli, alianza kutawala katika Samaria kwa miaka 41. Naye akafanya yaliyo maovu machoni pa BWANA. Mwana wake Yeroboamu Alisaidia kurudisha mipaka ya Israeli kama vile Yona nabii mwana wa Amitai alivyonena kama BWANA alivyomwambia. BWANA aliona mateso ya Waisraeli ni machungu sana na akawahurumia. Akarudisha Dameski na Hamathi. Yeroboamu akalala na baba zake na Zekaria mwanawe akatawala badala yake.

Katika mwaka wa 27 wa Yeroboamu mfalme wa Israeli, Uzia mwana Amazia mfalme wa Yuda alianza kutawala. Alikuwa na miaka 16 alipoanza kutawala na akatawala miaka 52. Huyu akafanya mema machoni pa BWANA ila mahali pa juu pa kutoa kafara kwa miungu migeni hapakuondolewa. BWANA akampiga ukoma mfalme hata siku ya kufa kwake, akakaa katika nyumba pekee ya kutengwa. Adhabu hii ilitokana na kufanya kazi ya kuhani. Uzia akalala na babaze na Yothamu akaanza kutawala.

Tusite hapa kidogo na kumwangalia Uzia, kijana mdogo wa miaka 16 ambaye anamrithi marehemu baba yake katika nafasi ya juu. Anafanya yaliyo sawa machoni pa Mungu. Anamtafuta Yeye Aliye Juu, na Bwana anamfanikisha. Kijana huyu ni mwenye akili, mbunifu, na mwenye nguvu 2 Mambo ya Nyakati 26. Yeye ni jasiri mbele ya upinzani, mjenzi wa miji, mpenda ardhi na ukulima. Kutoka tambarare hadi milima ushawishi wake unaonekana. Mifugo yake hulisha nyanda za chini, wakulima wake huchunga vilimani, na umaarufu wake unaenea mbali sana. Kijana anaiwezea teknolojia na ubunifu na kukuza rasilimali alizopewa. Anasaidiwa kwa jinsi ya ajabu na Mungu na anakuwa na nguvu nyingi. Je! unamfahamu mtu kama huyu aliyesoma vizuri au aliyefanya ujasiliamali toka utoto akafanikiwa sana? Au hata aliyerithi mali za wazazi naye akawa na kichwa kizuri na kujiepusha na uovu kabisa?

La kushangaza ni kwamba tunaambiwa baada ya mafanikio hayo. moyo wake ukajiinua kwa kiburi kwa sababu ya nguvu zake, na akampoteza Mungu ambaye Ndiye sababu haswa ya mafanikio yake! Mwanzo wa uharibifu wake umewadia sasa. Basi Akajichukulia mapendeleo au fursa ambayo hakuistahili, naye anakiuka moja kwa moja amri ya Mungu iliyo wazi wazi kabisa. Anakataa kutubu anapokemewa na anakatiliwa mbali na nyumba ya Bwana. Hatakuwa na heshima kutoka kwa Bwana tena. Je, wewe leo unmwona kijana anayehitaji ushauri wako wa kiroho ili kuepuka hatima ya kusikitisha kama ile ya Uzia?

Zekaria mwana wa Yeroboamu akatawala juu ya Israeli na Samaria kwa miezi sita. Alifanya maovu machoni pa BWANA, na kukosesha Israeli. Kisha Shalumu alifanya fitina naye akamwua mbele za watu. Basi lilitimia Neno la BWANA kwa Yehu kwamba wana wako watakaa kitini mpaka kizazi cha nne. Shalumu akaanza kutawala katika mwaka wa 39 wa Uzia mfalme wa Yuda, naye akatawala muda wa mwezi mmoja katika Samaria. Manahemu akapanda kutoka Tirza na kumwua, akatawala mahali pake.

*Kuungama Lazima Kuwe Mahususi (taja jambo lile kwa jina lake)—maungamo ya kweli daima ni ya tabia maalum, na hukiri dhambi fulani. Yanaweza kuwa ya namna ya kuletwa mbele za MUNGU tu na sio kwa binadamu wengi, yanaweza kuwa makosa ambayo yanapaswa kuungama mbele ya watu ambao wameumizwa majereraha kupitia kwazo, au yanaweza kuwa ya aina ya jumla ambayo yanapaswa kujulikana katika kusanyiko la watu. Lakini maungamo yote yanapaswa kuwa mahususi na mtu anapasa kwenda kwenye pointi/kipengele, yakikiri dhambi zote ambazo una hatia nazo.

---


Kwa nini wana wa Yehu walikaa kitini mpaka kizazi cha nne tu? Kwa nini mfalme Uzia alifukiza uvumba? Zekaria mwana wa Yeroboamu alitawala kwa muda gani? Je, Mfalme Uzia alijitwalia fursa gani?

**SIKU YA 140**
**(Mei 19)**

# Wafalme Zaidi

**- 2 Wafalme 15 na 2 Mambo ya Nyakati 28**

Katika mwaka wa thelathini na kenda wa Uzia mfalme wa Yuda, Menahemu mwana wa Gadi alianza kutawala juu ya Israeli, akatawala miaka kumi katika Samaria. Akafanya maovu machoni pa BWANA. Akaja Pulu mfalme wa Ashuru juu ya nchi, naye Menahemu akampa Pulu talanta elfu za fedha, ili ufalme wake uwe imara, kisha akawatoza watu wake kodi ili ampe mfalme wa Ashuru. Menahemu alipofariki Pekahia mwanawe alitawala pahali pake. Katika mwaka wa 50 wa Uzia mfalme wa Yuda, Pekahia alianza kutawala katika Samaria kwa miaka miwili. Akafanya maovu machoni pa BWANA. Na Peka jemadari wake akamfanyia fitina na kumpiga huko Samaria na kuchukua ufalme wake. Peka alianza kutawala katika Samaria mwaka wa 52 wa Uzia mfalme wa Yuda. Akafanya maovu machoni pa BWANA. Katika siku za Peka akaja Tiglath-pileseri mfalme wa Ashuru na kutwaa miji yake kama minane mfano Gileadi na Galilaya, akawahamisha watu kwake huko Ashuru. Hoshea, mfalme wa mwisho wa Israeli, akafanya fitina kwa Peka akamwua na kutawala mahali pake. Katika mwaka wa pili wa Peka, Yothamu mwana wa Uzia mfalme Yuda alianza kutawala, akiwa na umri wa miaka 25. Akafanya yaliyo mema machoni pa BWANA. Ila mahali pa juu hapakuondolewa, Yothamu akafa na Ahazi mwanawe akatalawa.



Ahazi mwana wa Yothamu mfalme wa Yuda alianza kutawala akiwa na miaka 20 na akatawala miaka 16. Wala hakufanya mema machoni pa BWANA. Hata akampitisha mwanawe motoni, sawasawa na machukizo ya mataifa yale BWANA aliowafukuza mbele ya wana wa Israeli. Akatoa uvumba katika mahali pa juu na chini ya miti mibichi. Resini mfalme wa Shamu na Peka mwana wa Remalia wa Israeli wakakwea juu ya Yerusalemu ili wapigane nao, ili wamhusuru Ahazi, lakini hawakuweza kumshinda. Basi Ahazi alituma ujumbe kwa Tiglath-pileseri mfalme wa Ashuru akasema, mimi ni mtumishi tena mwana wako; kwea ukaniokoe mkononi mwa mfalme wa Shamu na mkononi mwa mfalme wa Israeli, walioniinukia. Ahazi akafanya kosa la kutwaa dhahabu na fedha ya nyumba ya BWANA na kumpatia mfalme wa Ashuru kama zawadi ya kumtuliza. Mfalme wa Ashuru akasikia na akaenda kuutwaa Dameski, akawahamisha watu wake mateka, na kumwua Resini. Ahazi akaenda Dameski aonane na Tiglath-pileseri mfalme wa Ashuru, akaiona ile madhabahu iliyokuwa Dameski, kisha akamleta Uria kuhani aione ile madhabahu na kwa cheo chake akamwambia Uria aitengeneze. Ilipotengenezwa alikaribia karibu na kutoa sadaka.

Katika mwaka wa kumi na mbili wa Ahazi mfalme wa Yuda, Hoshea mwana wa Ela alianza kutawala Israeli na akafanya maovu machoni pa BWANA. Waisraeli waliwachukua Yuda mateka, na kuwaua wengine. Wengine walifanywa kuwa vijakazi wao. BWANA aliwaambia kupitia nabii Odedi, hata wao wana hatia zao hivyo wawarudishe ndugu zao Yuda, waliowachukua mateka. Basi watu wenye silaha waliacha wafungwa na nyara wakaondoka na kuwavika nguo waliokuwa uchi, wakawapa viatu na kuwalisha, wakawanywesha na kutia mafuta vidonda vyao. Basi wale dhaifu wakawapandisha punda na kuwaleta mpaka Yeriko, mji wa mitende kwa ndugu zao, kisha wakarudi Samaria. Majina ya mashujaa hawa waliofanya hisani ni vyema tuyajue, nayo ni Azaria, Berekia, Yehizikia, na Amasa. Mapigano haya yalileta mifarakano ya familia, na huzuni nyingi, kwani watoto walikuwa yatima, wanawake wajane, na kila mtu alitawanyika kila mahali.

Wengi wa wafalme hawa, ni baba pekee ndiye anayetajwa, lakini kwa wachache, mama zao wanatajwa! Cha ajabu, mama au mke anapotajwa, karibu kila mara hufuatwa na taarifa ya uaminifu wa mfalme. Ama, “Alifanya yaliyo mema machoni pa BWANA” au “Alifanya maovu mbele za BWANA.” Wengine hata wanaenda mbali zaidi, wakisema kwamba mfalme alifanya uovu kwa sababu mke au mama yake alimtia moyo katika njia hiyo! Hii inanionyesha uzito wa malezi ya mama kwa wema au ubaya, au ushawishi mzuri au mbaya wa mke!

Naye Shalmanesa mfalme wa Ashuru akakwea juu yake, Hoshea akawa mtumishi wake, akakwea Samaria na kuuhusuru miaka mitatu kwa vile alitegemea kodi kwa Hoshea naye hakuipata. Wana wa Israeli walipata shida hii kwa dhambi walizotenda kwa BWANA kwa kuchukua miungu mingine wakasahau BWANA aliyewatoa Misri. Walifanya mambo ya siri yasiyokuwa mema kwa BWANA wakaziendea njia za mataifa, wakitumikia sanamu na kufanya ibada za uovu, BWANA alizowakataza. Walifanya shingo zao kuwa ngumu, wakazikataa sheria zake na maagano yake, wakifuata ubatili. Wakapitisha watoto motoni ili kuwatoa kafara, wakapiga ramli, wakifanya uchawi, na kujiuza nafsi zao. Mfalme wa Ashuru

akaleta watu kutoka Babeli akawaweka katika miji ya Samaria badala ya wana wa Israeli. BWANA akaleta simba nao wakaua baadhi yao. Watu hawa wa Babeli walileta miungu yao, wakaendeleza machukizo ya kutoa watoto wao kafara kwa Adramaleki na Anameleki miungu yao bila kumwogopa BWANA.

Wazazi tunahitaji maombi mengi tunapopitia visa vya wafalme, kwani tunapokutana na ile hesabu ya siku ya mwisho yaani wakati wa hukumu, ni tukio lililoje litakaloonyeshwa pale! Maelfu ya watoto ambao wamekuwa watumwa wa ulafi katika kula na uovu mbaya kutokana na tamaa mbaya, ambao maisha yao yamekuwa ya uharibifu wa maadili. Hawa watasimama uso kwa uso na wazazi waliowafanya wawe vile walivyo. Ni nani isipokuwa wazazi wanapaswa kubeba Madaraka haya ya kutisha? Je, Bwana aliwafanya vijana hawa kuwa wafisadi? Jibu ni hapana! Ni nani, basi, amefanya kazi hii ya kutisha? Je! dhambi za wazazi hazikuambukizwa kwa watoto hawa kwenye tamaa ya hamu ya kula na tamaa za mwili potovu? Na je, kazi hii ya tabia haikukamilishwa na wale waliopuuza kuwalea au kuwazoeza kulingana na kielelezo ambacho Mungu ametoa? Kwa hakika kama walivyo, wazazi hao wote watatembelewa na kuonywa ila ni lazima tusikie/wasikie. Shetani yuko tayari kufanya kazi yake; hatapuuza kuwasilisha vivutio ambavyo watoto hawana nia au nguvu ya kimaadili kupinga. Kupitia vishawishi vyake, anaanzisha mitindo inayobadilika kila wakati, na karamu za kuvutia, ili akina mama waweze kuongozwa kutumia wakati wao kwa mambo ya kipuuzi, badala ya elimu na mafunzo ya watoto wao. Vijana wetu wanahitaji akina mama ambao watawafundisha kutoka utotoni kudhibiti matamanio, kukataa kuendeshwa na uchu wa chakula, na kushinda ubinafsi. Wanahitaji kuwa watu wa kanuni za ufalme wa Mungu.

Mama anapaswa kujaza nafasi ambayo Mungu alipanga kwa ajili yake awali. Ulimwengu unahitaji akina mama ambao ni mama jina tu, bali kwa kila maana ya neno. Tunaweza kusema kwa usalama kwamba kazi ya mwanamke ni takatifu. Hebu wakina mama watambue utakatifu wa kazi yao, na kwa nguvu na hofu ya Mungu wachukue utume wao wa maisha kwa umakini mwingi. Wawaelimishe watoto wao kwa manufaa katika ulimwengu huu, na kwa ajili ya makazi katika ulimwengu bora, wa mbinguni juu, ambao unakuja hivi karibuni! Kuna wengi hawana watoto ila wana nafasi kubwa ya kufanya tofauti kwa watoto ambao wanahitaji ushauri na malezi bora kwaajili ya upungufu fulani uliotokea, hata hivyo kijiji kizima au jamii yote inahusika na ukuaji bora wa mtoto.

Ninawasihi akina mama Waumini watambue wajibu wao, na kuishi, si kwa kujifurahisha wenyewe tu, si kwa kuwa kwenye simu, au mitindo, au maongezi, bali kumtukuza Mungu. Kristo hakujipendeza Mwenyewe, bali alichukua juu Yake namna ya mtumwa. Akaziacha nyua za kifalme, na kuuvika Umungu Wake ubinadamu, ili kwa mfano Wake Mwenyewe apate kutufundisha sisi jinsi tunavyoweza kuinuliwa hadi kwenye cheo kile cha wana na binti katika familia ya kifalme, watoto wa Mfalme wa mbinguni.

*Yesu Anasikia Ombi Rahisi la Msamaha—Sio lazima kwamba wote wataweza kubainisha kwa uhakika wakati dhambi zao ziliposamehewa. Somo la kufundishwa

kwa watoto ni kwamba dhambi na makosa yao vinapaswa kuletwa kwa Yesu katika maisha yao ya utotoni. Wafundishe kuomba msamaha Wake kila siku kwa kosa lolote walilofanya, na kwamba Yesu anasikia sala rahisi ya moyo uliotubu na wenye huzuni, Naye atasamehe, na kuyapokea, kama vile alivyowapokea watoto walioletwa Kwake alipokuwa duniani.

---

Kwa nini Menahemu alitoa dhahabu? Adramaleki ni nani? Nabii Odedi alitoa amri gani kutoka kwa BWANA? Tiglath-pileseri alikuwa ni nani? Je, pale unapoishi leo kuna miungu gani? Je, nasi tumesahau sheria, torati na amri alizotuandikia Mungu?

**SIKU YA 141**
**(Mei 20)**

# Makabila 10 ya Israeli Yalivyopotea

**- 2 Wafalme 15-17**



Ni vyema kuelewa kwamba nguvu na amani Israeli ilifurahia wakati Yeroboamu wa pili, ilikuwa ya muda mfupi, baada ya yeye kufa. Ufalme wake ulianza kupungua nguvu, na mtoto wake Zekaria akatawala miezi sita tu, na kuuwawa mbele ya watu na Shalumu ambaye alijitangaza kuwa mfalme. Lakini baada ya mwezi tu, Shalumu akauawa na Menahemu, aliyetawala kwa miaka 10 ya uovu mwingi na mateso kwa watu; wakitaabisha nchi, na kuchukua mema ya Israeli. Inaonekana wakati huo wafalme hawa wa Israeli walipata ufalme kwa kuwaua wengine, na wao pia wakauawa. Ikawa mkuki kwa mkuki, nchi ikataabika, na maadui wakazidi kushamiri wakishinda vita. Mabaya haya yote yalikuwa kwa Israeli kwa vile wao na wafame wao walimwacha Mungu wa baba zao na kuabudu miungu mingine au sanamu.

Hoshea alikuwa mfalme wa mwisho wa Israeli, yaani wa yale makabila kumi, na jumla kulikuwa na wafalme 19. Wakati wa Hoshea, Shalmanesa, mfalme wa Ashuru alikuja na jeshi kubwa mpaka Samaria na akauhusuru mji. Kuhusuru mji kulichukua miaka mitatu, na kuliisha kwa vile mfalme wa Ashuru, Shalmanese alifariki. Sargoni, jemedari wa jeshi akachukua kiti chake. Sargoni alimwua Hoshea mfalme wa mwisho wa Israeli na kuchukua watu wake kwenye nchi za mashariki kama vile Mesopotamia, Umedi na nchi za bahari ya Caspian. Sargoni alifanya hivi, ili apunguze nguvu za Israeli kumpinga.

Waisraeli katika nchi yao walikuwa wamemwacha BWANA na kuabudu miungu mingine, wakaenda mbali zaidi na kuanza kuabudu miungu ya watu wengine kule walikoishi. Wakaanza kuoa watu wa mataifa mengine, na hivyo wakakoma kuitwa Waisraeli. Walikuwa wamepoteza elimu au maarifa ya Mungu wao, aliyewapa Neno Lake na kuwatumia manabii. Hivyo ndivyo makabila yale kumi ya Israeli yalitokomea mpaka leo, hawakurudi tena katika nchi yao tena, bali walitawanyika katika mataifa mengine.

Mahali yalipoishi yale makabila kumi, mfalme wa Ashuru alileta watu wengine, na kwa sababu walikuwa wachache, wakaanza kupata shida ya wanyama wa mwitu kama simba kuwashambulia hawa wageni. Wale watu wakafikiri kwamba wanyama walikuja kwa sababu hawakumwabudu Mungu aliyetawala ile nchi. Kwa hiyo wakatuma ujumbe kwa mfalme wa Ashuru wakisema, tutumie kuhani, atakayetufundisha kawaida za Mungu wa nchi hii; kwa vile ameleta simba na wanatumaliza. Waliamini kwamba kila nchi ina Mungu wake. Wafilisti walimwabudu Dagoni, Wamoabu wakamwabudu Kemoshi, Watiro na Sidoni wakamwabudu Baali na Ashera. Hawakujua kwamba kuna Mungu mmoja tu anayetawala mbinguni na duniani, na ndiye Mwumbaji. Huyu anapaswa kuabudiwa na kila kiumbe.

Mfalme wa Ashuru alituma kuhani kutoka kwa wana wa Israeli, na akajaribu kuwafundisha watu kumcha na kumwabudu BWANA, iIa walipofanya ibada walichanganya ibada ya Mungu wa mbinguni na miungu yao. Hatuwezi kumwabudu Mungu tukichanganya changanya mambo. Kuna falme mbili tu, ufalme wa Mungu na ufalme wa Shetani. Basi watu hawa wakaitwa Wasamaria, kutokana na jina la mji wao mkuu wa Samaria ambao Ahabu aliuanzisha kama mji wake. Hawa walikuwa na hekalu lao, mlima wa Gerazimu karibu na mji wa Shekemu, hata leo katika mji huu kuna Wasamaria wachache.

*Kisha, watoto, njooni kwa Yesu. Mpe MUNGU sadaka ya thamani kuliko zote uwezavyo kutoa; mpe moyo wako. Anazungumza nawe akisema, “Mwanangu, binti yangu, Nipe moyo wako. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, nitazifanya nyeupe kama theluji; kwa maana nitawatakasa kwa damu yangu mwenyewe. Nitawafanya ninyi wanachama wa familia Yangu—watoto wa Mfalme wa mbinguni. Pokeeni msamaha Wangu, Amani Yangu ninayowapa ninyi bure. Nitawavika ninyi kwa haki Yangu, vazi la harusi, na kuwafanya mstahili karamu ya harusi ya Mwana-Kondoo. Mnapovikwa haki Yangu, kwa maombi, kwa kukesha, kupitia kujifunza Neno Langu kwa bidii, mtaweza kufikia kiwango cha juu. Mtaelewa Ukweli, na tabia yenu itaundwa/itafinyangwa na ushawishi wa Bwana; “Ombeni kwa ajili ya Msamaha kwani haya ni mapenzi ya MUNGU, hata kutakaswa kwenu.”

---

Umejifunza nini katika historia hii? Makabila 10 ya Israeli yalipoteaje? Kwa nini hatuwezi kumwabudu Mungu na miungu mingine? Kwa nini Wayahudi na Wasamaria walichukiana? Soma Yohana sura ya 4.

**SIKU YA 142**
**(Mei 21)**

# Mfalme Hezekia Afanya Israeli Imrudie Mungu kwa Matengenezo na Uamsho

**- 2 Wafalme 18-19; 2 Mambo ya Nyakati 29-32; Isaya 36-37**



Ikawa katika mwaka wa tatu wa Hoshea mfalme wa Israeli, Hezekia mwana wa Ahazi akawa mfalme wa Yuda. Mama yake Hezekia aliitwa Abiya, naye alikuwa binti wa Zekaria, nabii aliyeuawa na mfalme Yoashi. Hivyo Hezekia mfalme alikuwa mjukuu wa Yehoyada kuhani mkuu na kitukuu cha Athalia! Alikuwa na miaka 25 alipoanza kutawala, na akatawala miaka 29. Akafanya mema mbele za BWANA. Akapaondoa pahali pa juu, akazibomoa nguzo za Ashera, akamvunja vipande yule nyoka wa Shaba ambaye Musa alimfanya jangwani. Hii ni kwa vile watu walianza kumwabudu wakifukiza uvumba kwake. Naye akamuita Nehushtani. Alimtumaini Mungu japo alikuwa na baba na mababu waovu. Hakuna mfalme wa Yuda aliyeshikama na Mungu kama huyu, kwani hakuacha kumfuata BWANA. Naamini mama yake alikuwa na sehemu kuhusu wongofu wake. Hezekia akawaagiza makuhani na Walawi wajitakase na kutoa uchafu katika patakatifu. Akawaambia makuhani BWANA amewachagua ninyi msimame mbele yake, kumhudumia, na kuwa watumishi wake. Wakasikiliza ushauri, nao wakatoa dhabihu kwa BWANA wakashika sheria za Musa. Akasafisha nyumba ya BWANA na kila alikokwenda alifanikiwa. Akawapiga Wafilisti mpaka Gaza na mipaka yake.

Hezekia Alirudisha huduma ya nyimbo, vinanda na mapanda kama vile nabii Nathani na Gadi walivyosema. Walipotoa sadaka za kuteketezwa wakaanza na wimbo wa Bwana. Watu wengi walikuwa tayari kutoa sadaka hata wengine waliorudi nyuma wakaanza kurudisha zaka. Uamsho na Matengenezo kwa mambo ya kiroho

vilifanyika. Hezekia akatuma watu katika Yuda kuwaambia watu warudi kwa Mungu wa Ibrahimu, na Isaka na Yakobo. Hakika hali ya kiroho ya watu kwa kawaida haiwi juu ya viongozi wao. Watu waliitwa kula Pasaka, wengine hawakufuata sheria. Hezekia akawaombea kwa Mungu ili awasamehe kwa sababu hawajui. Walikuwa wamekaa muda mrefu na mambo ya giza, lakini kwa kuwa walikaza kutafuta kwa moyo wao wote, wasamehewe, na Mungu akasikia. Ni upendo kuwapenda wenzetu na kuwaombea. TOA UCHAFU KUTOKA MAHALI PATAKATIFU. Tunawashukuru sana viongozi walio vijana, ambao ni jasiri ambao wako tayari kuchukua msimamo kwa ajili ya BWANA. Wengi waliofanya matengenezo ya kanisa katika historia ya dunia, walikuwa vijana wa kiume na wa kike, na waliposimama kwa ujasiri dhidi ya ufisadi na ukengeufu wa Kanisa Bwana aliwashindia. Katika harakati zetu wenyewe za kanisa la Masalio, viongozi wengi walikuwa vijana chini ya miaka 26. Twashukuru viongozi walio vijana leo katika eneo la huduma ya uinjilisti wa vyombo vya habari, ambao wako tayari kuchukua msimamo kwa ajili ya BWANA. Tuwaombee viongozi wetu wote hasa vijana ambao BWANA anaendelea kuwainua katika siku hizi za mwisho. Hili hapa ni swali langu kwako na kwangu leo: Ni uchafu gani tunaopaswa kutekeleza kutoka mahali Patakatifu katika siku zetu? Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu, Je, kuna kile ambacho tunapaswa kukiacha ili kulifanya Hekalu la miili yetu kuwa safi?

Abiya, mama wa Hezekia alikuwa binti wa nabii Zekaria. Yawezekana ndiye aliyechangia tabia ya mfalme huyu. Watoto ni washiriki wachanga wa familia ya Mungu, waliokabidhiwa kwa wazazi ili kuelimishwa kwa hekima, na kuadabishwa kwa uvumilivu ili waweze kuunda tabia za mbinguni, na kustahiki kubariki wengine katika maisha haya, na kufurahia maisha yajayo. Uhusiano nyeti zaidi wa kidunia ni ule kati ya mama na mtoto wake. Mtoto huvutiwa kwa urahisi zaidi na maisha na mfano wa mama kuliko ule wa baba, kwa kuwa kifungo chenye nguvu na nyororo zaidi cha muunganiko huwafunga hao wawili. Mawazo na hisia za mama zitakuwa na ushawishi mkubwa juu ya urithi anaompa mtoto wake. Ikiwa ataruhusu akili yake ikazie juu ya hisia zake mwenyewe, ikiwa anajiingiza katika ubinafsi, ikiwa ni mnyonge na mwenye kulazimisha mambo kwa ukali, tabia ya mtoto wake itashuhudia ukweli huo. Hivyo wengi wamepokea kama urithi wao mielekeo isiyoweza kushinda uovu. Adui wa roho anaelewa jambo hili vizuri zaidi kuliko wazazi wengi. Ataleta majaribu yake juu ya mama, akijua kwamba ikiwa hatampinga, anaweza kumuathiri mtoto wake kupitia yeye. Tumaini pekee la mama ni kwa Mungu. Anaweza kumkimbilia Bwana kwa nguvu na neema; naye hatatoka bure. Mama Mkristo atakuwa macho ili kutambua hatari zinazowazunguka watoto wake. Ataiweka nafsi yake katika hali safi, na takatifu; na kisha atadhibiti hasira yake na kanuni zake kwa Neno la Mungu, naye atafanya wajibu wake kwa uaminifu, akishinda majaribu madogo na makubwa ambayo yatamshambulia daima.

Mwaka wa 14 wa Hezekia, Senakeribu, mfalme wa Ashuru akaja Yuda kupigana na kuitwaa miji yao. Hezekia alituma ujumbe kwa mfalme wa Ashuru akisema, “Nimekosa uniache ukarudi kwako.” Akamwambia kuwa cho chote atakachotaka atampa, na mfalme wa Ashuru akawatoza kodi talanta za fedha mia tatu na za dhahabu thelathini. Hezekia akampa fedha na dhahabu za nyumba ya BWANA na katika hazina za nyumba ya mfalme. Hii haikusaidia, kwani mfalme wa Ashuru

akataka zaidi, akawatuma jemedari wake na mkuu wa matowashi wakakwea Yerusalemu, wakaja na kusimama karibu na mfereji wa birika la juu. Wakamwita mfalme, na Eliakimu msimamizi wa nyumba ya mfalme, Shebna mwandishi na Yoa mwenye kuandika tarehe na rekodi wakaja pia. Amiri wa Ashuru akatoa ujumbe toka kwa mfalme, kwamba Hezekia ana matumaini gani hata akamwasi bila kulipa ushuru? Kwa dharau akasema hakuna atakayeweza kumsaidia Hezekia dhidi yake. Kama ni Wamisri anawatumainia, hawa ni kama fimbo ya mwanzi uliopondeka. Hata BWANA wa Israeli hatawasaidia. Akasema BWANA Ndiye amemwambia, “panda upigane na nchi hii na kuiangamiza.” Wale wajumbe wa Hezekia wakamsihi yule jemedari wa Ashuru azungume Kiashuru ili raia wa Yuda wasisikie na mfalme asiaibike. Bali yule jemedari alijibu kwa ujeuri kwa Kiyahudi ili wale watu wa ukutani waipate!, “Je! Hakunituma ili watu hawa walio ukutani wale mavi yao wenyewe na kunywa mkono wao pamoja nanyi?” Basi yule jemedari akapiga kelele akisema, “Lisikieni neno la mfalme mkuu wa Ashuru… Hezekia asiwadanganye kwa maana hataweza kuwaokoa katika mkono wake. Wala Hezekia asiwatumainishe katika BWANA akisema hakika BWANA atatuokoa, wala mji huu hautatiwa mkononi mwa mfalme wa Ashuru … Fanyeni suluhu na mimi, mkatoke mnijie; mkale kila mtu matunda ya mzabibu wake na matunda ya mtini wake, … ili mpate kuishi msife, wala msimsikilize Hezekia awadanganyapo… Je, yupo mungu mmoja wa mataifa aliyewaokoa watu wake wakati wowote na mkono wa mfalme wa Ashuru?”

Watu wa ukutani na wale viongozi walinyamaza kimya, wala hawakumjibu neno lolote, kama vile mfalme alivyowaambia. Kisha walienda kwa Hezekia nguo zao zimeraruliwa, na kumpa ujumbe wa yule amiri. Naye mfalme aliposikia maneno hayo alizirarua nguo zake akajivika magunia na kuingia nyumbani mwa BWANA. Akatuma wazee na makuhani wajivike magunia, waende kwa Isaya nabii wamwambie, “Siku hii ni siku ya dhiki na aibu na matukano, maana watoto wa tayari kuzaliwa, wala hapa nguvu ya kuwazaa.” Walakini Mungu asikie maneno ya Amiri huyu, ambaye mfalme wake wa Ashuru amemtuma amtukane Mungu aliye hai, naye atayakamea hayo maneno aliyoyasikia.” Akampa ujumbe Isaya ainue dua kwa Mungu. Isaya akarudisha ujumbe akisema, “usiyaogope maneno hayo uliyoyasikia … Tazama nitatia roho ya hofu ndani yake, naye atasikia kivumi, na kuirudia nchi yake mwenyewe, nami nitamwangusha kwa upanga katika nchi yake mwenyewe.”

Mfalme wa Ashuru alituma ujumbe tena wa pili, “Mwambieni Hezekia mfalme wa Yuda maneno haya, mkisema, asikudanganye Mungu wako unayemtumaini, akisema Yerusalemu hautatiwa katika mikono ya mfalme wa Ashuru.” Akawatia hofu Yuda kwamba amepiga nchi nyingi, “Je, utaokoka wewe?” Akaanza kutaja nchi alizozipiga.

Hezekia alipokea waraka wa mfalme wa Ashuru na alipousoma, akaingia nyumbani mwa BWANA na kukunjua ile barua, mbele za BWANA na akaomba, akisema, “Wewe ukaaye juu ya makerubi, Wewe peke yako, Ndiwe Mungu wa falme zote za dunia, Wewe Ndiwe uliyeziumba mbingu na nchi. Tega sikio lako, Ee BWANA… uyasikie maneno ya Senakeribu …” kumtukana Mungu Aliye Hai. Ni kweli wameharibu

nchi nyingi na kuitupa miungu yao kwa vile haikuwa miungu. "Basi sasa Ee Bwana Mungu wetu utuokoe na mkono wake tunakusihi, ili falme zote za dunia zipate kujua ya kuwa wewe ndiwe BWANA Mungu, wewe peke yako." Isaya nabii akaja na ujumbe kwa mfalme Hezekia, kwamba kwa vile ameomba, basi BWANA amesikia. Maana mfalme wa Ashuru hakuinua sauti kwa Hezekia bali kwa Mtakatifu wa Israeli. Kwa vinywa vya wajumbe amemshutumu BWANA akijisifia magari yake, yakienda Lebanoni na kwenye kuikata mierezi na misonobari mizuri. Amejisifu kukausha maji ya Misri, je, mfalme wa Ashuru hakusikia kwamba BWANA Ndiye ametenda maajabu hayo tokea zamani za kale? "kwa sababu ya kujisifu kwako, nakujua kuketi kwako na kutoka kwako, kujisifu kwako kumefika masikioni mwangu, Nami nitatia kulabu puani mwako na hatamu mdomoni mwako, Nami nitakurudisha kwa njia ile uliyoijia. BWANA akamwambia Isaya amwambie mfalme Hezekia, "Hatauingia mji huu, wala hatapiga mshale hapa, wala hatakuja mbele yake kwa ngao, wala hatajenga boma juu yake… njia ile aliyoijia, kwa njia hiyo hiyo atarudi zake… maana nitaulinda mji huu niuokoe, kwa ajili Yangu Mwenyewe na kwa ajili ya mtumishi Wangu Daudi." Siku hiyo hiyo malaika wa BWANA aliingia na kuwapiga Waashuru 185,000 na watu walipoamka walikuta maiti hizo. Senakeribu mfalme wao, akarudi amenywea na kukaa Ninawi. Ikawa alipokuwa akiabudu mungu wake, Adramaleki na Sharezi wana zake wa kuzaa, wakampiga kwa upanga na kukimbilia nchi ya Ararati. Esar-hadoni mwana wake akatawala mahali pake. Hakika Mungu ajaibu mambo ya waja Wake.

*Ombi la Msamaha Lazima Lionyeshwe Kuwa la Unyofu (litoke moyoni)— "Usinitenge na uso wako, wala usimwondoe Roho wako Mtakatifu." Toba pamoja na msamaha ni zawadi ya MUNGU kupitia Masihi. Ni kupitia ushawishi wa Roho Mtakatifu ndipo tunasadikishwa kuhusu dhambi, na kuhisi hitaji letu la msamaha. Hakuna wanaosamehewa isipokuwa wale walio na moyo uliopondeka; lakini ni neema ya Bwana ifanyayo moyo kutubu. Anafahamu udhaifu na mapungufu yetu wote, Naye atatusaidia. Atasikia maombi ya imani; lakini unyoofu wa sala unaweza kuthibitishwa tu kwa jitihada zetu za kujileta kwenye mapatano na kile kiwango kikuu cha maadili ambacho kitapima tabia ya kila mtu (Amri Zake Kumi). Tunahitaji kufungua mioyo yetu kwa ajili ya ushawishi wa Roho, na kupata uzoefu wa nguvu Zake zinazobadilisha.

---

Kwa nini hongo ya kumpa mfalme wa Ashuru vitu vya nyumba ya BWANA ilikuwa ni kosa? Hezekia alipopokea waraka alifanyaje? Mama ya Hezekia aliitwa nani? Waashuri 185,000 walikufaje? Ni mambo gani mazuri ambayo mfalme Hezekia alifanya? Leo hatusherekie Pasaka ila tunasherekea meza ya Bwana, unaweza kuelezea tofauti kati ya sakramenti hizi mbili?

**SIKU YA 143**
**(Mei 22)**

# Kuugua kwa Hezekia na Jua kusimama

**- 2 Wafalme 20; 2 Mambo ya Nyakati 29-32; Isaya 38-39**




Basi Hezekia akaugua akawa katika hatari ya kufa. Isaya mwana wa Amozi nabii akamjia akamwambia atengeneze mambo ya nyumba yake maana atakufa wala hatapona. Basi Hezekia akasikitika na kugeuza uso wake, akamwomba BWANA akielekeza uso wake ukutani kwa machozi mengi. Hezekia akaomba akisema, "Nakusihi, BWANA, ukumbuke sasa jinsi nilivyokwenda mbele Zako katika kweli na kwa moyo mkamilifu na kutenda yaliyo mema machoni pako." Ikawa kabla Isaya hajatoka katika mji, Neno la BWANA likamjia arudi kwa Hezekia na kumwambia BWANA asema hivi, nimeyasikia maombi yako, na kuyaona machozi yako; tazama, nitakuponya; siku ya tatu utapanda nyumbani mwa BWANA."

BWANA akaahidi kuzidisha siku za Hezekia kwa miaka 15 na kumwokoa yeye na mji, na mkono wa mfalme wa Ashuru na kuulinda mji, kwa ajili yake BWANA na mtumishi Wake Daudi. Isaya akamwambia atwae mkate wa tini, kiwe kama kibandiko kuweka kwenye jipu ambalo ndilo lilikuwa ugonjwa wake. Mungu alitumia tiba mbadala, hata wengine nimeona wakiweka viazi ulaya au kitunguu kilichosagwa kuwa dawa ya kunyonya sumu au kupunguza maumivu ya jipu, mahali penye shida au palipovimba. Mungu anao uweza wa kuponya bila hivi, lakini mara nyingine anataka tutumie tiba mbadala au tiba rasmi za hospitali. Mara zingine anataka tufanye mazoezi, tunywe maji, tupate mwanga wa jua au kula chakula bora. Basi mfalme alipofanya hivi alipona, na Isaya akamwambia achague ishara ya kivuli kwenda mbele au kurudi nyuma. Naye Hezekia akachagua "kivuli kirudi nyuma madaraja kumi." Isaya akamlilia BWANA na kivuli kikaenda nyuma madaraja kumi.

Tukiombea wagonjwa tusivuke mipaka na kuwa na harakati tunazoziita 'kutochukua dawa ni imani' wakati ni dhana. Kuna wakati inabidi tutumie tiba kama Hezekia alipoambiwa kutumia makuyu. Pia kuna wakati tunahitaji hekima ya kumwambia Mungu mapenzi Yake yatimizwe na si yetu, kwani kuna wengine wakirudishiwa afya, huishi maisha ya uovu sana, wakati ambapo wangepumzika wangeweza kuingia mbinguni siku moja.

Ikiwa watachukua msimamo kwamba katika kuombea uponyaji lazima wasitumie tiba rahisi zinazotolewa na Mungu ili kupunguza maumivu na kusaidia asili katika kazi yake, isije ikawa ni kukana imani, wanachukua nafasi isiyo ya busara. Huku si kukana imani; bali kupatana kabisa na mipango ya Mungu. Hezekia alipokuwa mgonjwa, nabii wa Mungu alimletea ujumbe kwamba lazima afe. Alimwinua Bwana, na Bwana akamsikia mtumishi wake na kufanya muujiza kwa niaba yake, akimpelekea ujumbe kwamba miaka kumi na mitano ingeongezwa kwa maisha yake. Sasa, Neno moja kutoka kwa Mungu, mguso mmoja wa kidole cha Mungu, ungemponya Hezekia mara moja, lakini maagizo maalum yalitolewa kuchukua mtini na kuuweka juu ya sehemu iliyoathirika, na Hezekia akafufuliwa. Katika kila jambo tunahitaji kwenda kwenye mstari wa majaliwa ya Mungu.



Wakati huo Merodak-baladani mfalme wa Babeli, alituma zawadi kwa Hezekia kwa maana alipata habari kwamba Hezekia aliugua na akapona. Hezekia akafanya kosa kwani badala ya kumtukuza Mungu mbele za hawa Wababeli, yeye aliwaonesha fahari ya nyumba na hazina yake. Aliwaonesha vitu vyake vya thamani, fedha, dhahabu, manukato, marhamu, nyumba ya silaha, na vitu vyote vilivyoonekana katika hazina yake. Wala hapakuwa na kitu asichowaonesha Hezekia katika nyumba yake, katika ufalme wake wote. Ndipo nabii Isaya akamwendea na kumwambia wale wageni wametoka wapi? Akajibu wametoka katika nchi ya mbali, yaani Babeli. Akaendelea kuuliza, "wameona nini nyumbani mwako?" Hezekia akajibu kwamba vitu vyote amewaonesha, hakuna alichoficha katika hazina yake. Mungu alimfanyia mwujiza wa kumponya ugonjwa wa kufa. Mfalme wa Babeli asiyekuwa mcha Mungu alioneshwa hazina na fahari za mfalme Hezekia huku akijigamba kwa vitu alivyo navyo badala ya kutoa ushuhuda wa mambo makuu ambayo Mungu alikuwa amemfanyia kwa kumwokoa na Waashuru na kwa kumponya ugonjwa, na hata mwujiza wa kivuli kurudi nyuma madaraja kumi na tano, ambao ndio uliomvuta mfalme wa Babeli kutuma wajumbe. Haya yote hakuyaeleza ila alionyesha vitu vyake. Hata leo tunapewa nafasi kueleza matendo makuu na upendo wa Mungu kwa marafiki zetu, majirani na hata ndugu, lakini mara zingine tunaonyesha vitu tulivyo navyo. Hili ni kosa, tumuombe Mungu

atusaidie tusiingie katika shimo hilo. Wengine wanapoponywa ugonjwa na Mungu humpa sifa zaidi tabibu wao kwamba ni bingwa, au hujigamba kuhusu bidii zao za tiba mbadala. Wengine wakipata kazi baada ya kutafuta kwa muda mrefu, huweza kusema ni kisomo chao kikubwa, ujanja wao, au ni jamaa yao ambaye ni bosi amewasaidia pale, japokuwa huenda kwa miaka minne walikuwa na nyenzo zote hizo ila hazikufua dafu. Katika yote lazima Mungu arudishiwe utukufu anaostahili, tunaweza kuwaonyesha watu majumba yetu, ila si kwa kujigamba.

Isaya akamwambia Hezekia kuwa hilo ni kosa, na siku zinakuja Wababeli watakuja na kuchukua vitu hivi vyote mpaka Babeli. Watachukua wana wake mbali, nao watakuwa matowashi nyumbani mwa mfalme wa Babeli. Hezekia akakubali adhabu ya Mungu, ila alisema adhabu hiyo ni sawa na ije wakati yeye amekufa. Maskini mfalme huyu alikuwa radhi kumwachia mtoto wake adhabu zake, badala ya kujikaza kisabuni na kuzichukua mwenyewe.

Hezekia alifanya matengenezo makubwa, hata Walawi walianza kuwa na zamu na kuendelea na ibada inavyotakiwa. Makuhani wakawabariki watu, ikasikiwa sauti yao, na sala yao ikafika hata makao yake matakatifu, yaani mbinguni. Watu walitoa sadaka za asubuhi na jioni, sadaka za sabato, mwezi mpya, zaka, na kujibidisha. Kuhani mkuu Azaria aligundua kuwa, "tangu watu walipoanza kuleta matoleo nyumbani mwa BWANA, walikula na kushiba na kusaza tele. BWANA alikuwa amewabariki watu Wake kwa wingi. Hezekia alikuwa na heshima, mali, chakula, vinywaji, vito, na mifugo tele. Ili watu waweze kufanya matengenenezo wanahitaji neema na furaha, watoto wa Mungu tunapaswa kuondoa sanamu za miungu yetu mioyoni, nyumbani mwetu, na kwenye makanisa yetu. Sanamu haziondolewi moyoni hadi tumekuwa na wakati wa ibada na shangwe au kufurahia. Inaonekana kuna ukweli kwenye akili zetu kwa mpangilio huu wa matukio. Mioyo yenye shangwe hushikamana na moyo wa Mungu na kusalimisha sanamu zake. Pale ambapo kuna furaha kidogo, kuna uamsho mdogo. Ndivyo ilivyo hivi leo: Maisha yanapojaa shangwe na kupendeza, watu hubomoa sanamu zilizooza mioyo mwao, sanamu za ubinafsi, michezo, chakula, chuki, maoni, simu, media, urembo, vyeo, elimu, ponografia. . . au chochote kile ambacho ni sanamu yetu kipenzi inaweza kuwa. Hezekia alitoa ahadi nzuri: "Mungu hataugeuza uso Wake kutoka kwenu mkimrudia Yeye." Mungu hamwaibishi wala kumkataa mtu yeyote anayetubu! Badala ya kutuacha/kuniacha, Yeye atakugeukia/atanigeukia wewe/mimi kwa moyo wa neema na shangwe kama ilivyokuwa kwa mwana mpotevu. Mwito wa toba lazima daima uambatanishwe na uhakikisho wa neema na furaha/shangwe. Kuna furaha mbinguni kwa mwenye dhambi mmoja tu anaporudi zizini! Mungu alimtoa Mwanawe ili tuokolewe na siyo tuangamie, ndiyo jambo la kukumbuka daima.

Mtu anaweza kuuliza kama miaka ya ziada ya Hezekia ilikuwa mbaraka kweli? Endapo angekufa wakati ambao Mungu alikuwa ameweka hapo awali, hangemzaa Manase. Kifo cha kijana ni kichungu sana, lakini ikiwa mtu huyo alikuwa ndani ya Kristo, tunapaswa kuamini kile ambacho Biblia inasema kwamba, "wenye haki hupotea/hufa, wala hakuna atiaye hayo moyoni; na watu watauwa huondolewa, wala hakuna afikiriye ya kuwa mwenye haki ameondolewa asipatikane na mabaya.." Isaya 57:1

Wazazi tujifunze ili yakitusibu haya yaliyomtokea mfalme huyu tusiwe tayari kusema watoto wetu wapokee adhabu za uovu wetu. Kwamba ni sawa watoto wetu wapate laana, ila kwetu wenyewe si sawa! Basi Hezekia alifariki na mwanawe Manase alitawala mahali pake.

*Ni muhimu sana kwamba tunapaswa kuomba ili tupate nguvu kutoka juu ya kuyaona na kuyapinga majaribu ya adui; lakini Shetani hutafuta siku zote kuwazuia watu wasiombe, kwa kuujaza muda wao kwa biashara, biashara au starehe, au kwa kuwaongoza katika uovu wa namna hiyo hata wasiwe na hamu ya kuomba. Bwana Yesu amefanya mbingu ifikike kwa wote wanaoenda Kwake, na anawaalika watoto na vijana waje Kwake. Akisema, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie; kwa maana ufalme wa MUNGU ni wao." Yesu angetaka watoto na vijana waje Kwake wakiwa na ujasiri ule ule wanaoenda nao kwa wazazi wao. Kama vile mtoto anavyomuomba mama yake au baba yake chakula akiwa na njaa, ndivyo Bwana anavyotaka ninyi muombe kile mnachohitaji. Ikiwa dhambi zako ni nzito juu ya moyo wako, unapaswa kwenda kwa MUNGU na kusema, "Kwa ajili ya Masihi, nisamehe dhambi zangu." Kila sala ya unyoofu itasikiwa mbinguni, na kila ombi la dhati na bidii la neema na nguvu litajibiwa.

---

Hezekia alipougua aliambiwa atumie dawa gani? Alipewa miaka mingapi ya kuishi? Hezekia alifanya dhambi gani? Marafiki zako wakija nyumbani kwako leo utawaonesha nini? Unawezaje kumpa Mungu utukufu kwa mambo anayokutendea?

**SIKU YA 144**
**(Mei 23)**

# Mfalme Manase na Yosia

**- 2 Wafalme 21; 2 Mambo ya Nyakati 33**



Manase alianza kutawala akiwa na miaka 12 na akatawala miaka 55. Alitawala muda mrefu kuliko wafalme wote wa Israeli. Naye ndiye aliyekuwa mfalme mwovu kupita wote waliotawala Yuda. Alizaliwa katika ile miaka 15 babaye aliyoomba nyongeza. Wengine wamesema kuwa pengine kama Hezekia angekubali kupumzika asiishi ile miaka 15, mtoto wake Manase asingezaliwa na kuleta huzuni kubwa kwa wengi na kwa Mungu pia. Wengi aliowapoteza, yeye aliporudi kwa BWANA wao walipotea milele, hii inaonesha mvuto mzito wa uongozi. Manase alifanya machukizo, na kujenga mahali pa kufukiza uvumba kwa miungu mingine, akajenga madhabahu ya Baali na maashera ambayo baba yake aliyabomoa. Akampitisha mwanawe motoni, akatazama bao, akafanya uganga, akajishugulisha na pepo wa utambuzi, na wachawi, na kumkasirisha BWANA. Aliweka sanamu ya kuchonga ya Ashera ndani ya nyumba ya Mungu. Manase akawakosesha Yuda na Yerusalemu mbele za Mungu. manase akamwaga damu zisizo na hatia, nyingi sana. Wanahistoria wanasema akamwua hata nabii Isaya kwa kumkata vipande viwili na msumeno. Nabii ambaye alimtumikia baba yake kwa uaminifu. Acheni Mungu aitwe Mungu, ni mwenye huruma, si mwingi wa hasira, na mwepesi wa kusamehe, tukiungama na kuwa na toba ya kweli.
Kuwa kiongozi ni wito ulio mtakatifu na wa juu sana, Manase alivutiwa na kuabudu sanamu. Leo ibada za sanamu ni nyingi: kupenda pesa, ulafi wa chakula, kucheza michezo ya video, mitandao ya kijamii, kupoteza muda katika kutazama burudani zisizo na maana kwenye televisheni au mtandao, kuwa kwenye simu saa yote, kiburi cha cheo, kuabudu fasheni, elimu, maoni na mahaba yaliyopigwa marufuku. Hakika tabia yoyote inayoharibu afya ambayo inatufanya tufeli ni sanamu. Hebu tuutafute kwanza ufalme wa Mungu na haki Yake.

Manase alirudi kwa BWANA, na BWANA akampokea kwa kuwa Yeye ni Mwenye huruma. Kama Wewe BWANA ungeyahesabu makosa, ni nani angesimama? Lakini Kwako kuna msamaha ili wewe uogopwe. Manase alirudi baada ya kupata adhabu, ila alikuwa amepotosha wengi, ambao walikwenda dhambini moja kwa moja, bila kurudi kwa BWANA kama yeye. Na hili ni somo la kujifunza kwamba dhambi

zetu, hata tukiacha, tunakuwa tumeweka harufu na mvuto, kwa kuwakosesha au kuwakwaza wengine milele.

Manase alichukuliwa na ndoana kwenye pua kama mnyama na mateka na mfalme wa Ashuru mpaka Babeli. Alipokuwa katika taabu, kiburi kilishuka na akamlilia Mungu na kumsihi akijinyenyekeza ili akubaliwe. Akamkumbuka baba yake, shujaa aliyempenda Mungu, na kuungama. Mungu akasikia maombi yake na kumrudisha Yerusalemu tena, ndipo akajua kwamba BWANA Ndiye Mungu. Basi akaondoa miungu migeni, na kutoa sadaka za shukurani na kuwaambia watu wamfuate BWANA.

Manase alipokufa, mwanawe Amoni akatawala mahali pake akiwa na miaka 22. Akafanya yaliyo maovu machoni pa BWANA kama babaye Manase. Watumishi wa Amoni wakafanya fitina na wakamwua mfalme ndani ya nyumba yake mwenyewe. Watu wa nchi wakalipiza kwa kuwaua wale wote waliomwua Amoni, na kumfanya Yosia, mtoto wake wa miaka nane kutawala. Huyu alitawala miaka thelathini. Japo alikuwa mdogo, Yosia akafanya yaliyo mema kama Daudi babaye, hakugeuka kuume wala kushoto. Ikawa katika mwaka wa kumi na nane wa Yosia, alimtuma Shafani, mwandishi nyumbani mwa BWANA ili aende kwa Hilkia, kuhani mkuu, waihesabu sadaka watu walioyoleta kupitia kwa walinzi. Kisha waichukue hiyo pesa na kukarabati hekalu, mahali palipobomoka. Maseremala, wajenzi, na waashi, wakanunua miti, mawe yaliyochongwa ili wapate kutengeneza nyumba.

Hilkia kuhani akamwambia Shafani mwandishi, kwamba amekiona kitabu cha torati katika nyumba ya BWANA. Akampa ili akisome. Shafani akafika kwa mfalme na kumwambia wamezitoa zile fedha, na kukabidhi wafanyakazi wanaosimamia nyumba ya BWANA. Kisha Shafani mwandishi akamwambia mfalme kuhusu kitabu alichopewa na Hilkia kuhani. Shafani alipokisoma mbele ya mfalme, mfalme alirarua nguo zake, akaamuru kuhani Hilkia na wenzake waliokuwa kwenye uongozi wa mambo ya Kiroho waende wakaulize kwa BWANA kwa ajili yake mfalme, na kwa ajili ya raia wote, katika habari ya maneno ya kitabu kilichoonekana hekaluni. Mfalme akasema, kwa kuwa hasira ya BWANA ni kubwa aliyotukasirikia katika habari ya Maneno ya kitabu kilichoonekana. Basi Hilkia kuhani na wenzake wakamwendea Hulda nabii mke na kumwuliza. Hulda nabii akajibu, BWANA asema hivi, Tazama mimi nitaleta uovu juu ya mahali hapa, na juu yao wakaao hapa na maneno yote ya kitabu alichokisoma mfalme wa Yuda. Kwa sababu wameniacha mimi, na kufukiza uvumba kwa miungu mingine ili wapate kunikasirisha kwa kazi yote ya mikono yao. Ila akasema kwa vile mfalme wa Yuda moyo wake umekuwa mwororo kusikia, kisha akajinyenyekeza mbele ya BWANA aliposikia maneno hayo, na akazirarua nguo zako, na akalia mbele za BWANA, basi BWANA alimsikia. Sadaka bora kwa BWANA ni moyo ulipondeka na kunyenyekea, tukiwa tayari kuungama makosa yetu na ya wenzetu. Moyo uliopondeka, BWANA hataudharau. Kuna wengi wanaoonekana hawana dhambi kubwa, ila dhambi ya kiburi ni kubwa sana, hii hairuhusu neema ya Mungu kufanya kazi. Mtu anakataa kutubu, na yule ambaye amekuwa mbaya sana hata kuua, husamehewa kwa vile amekuwa na toba ya kweli na kujinyenyekeza. Basi Yosia akaahidiwa kuwa hataona uovu wote BWANA atakaouleta kutokana na maovu bali atapumzika kaburini na baba zake.

Tunapata fundisho hapa kuhusu umuhimu wa Maandiko Matakatifu, na kuyasoma ili tujue Mungu anataka nini toka kwetu. Hili itabadilisha maisha yetu, kwa kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu na kuwa na upendo kwa watu. Kusoma Biblia ni kama kutungua matunda kwenye mti wa machungwa. Unaanza kutingisha mti wote, kisha matawi na kisha kwenye tunda lenyewe! Hebu tuanze leo kutingisha ili tupate matunda matamu kwenye mti wa Neno Takatifu.
Mambo ya Nyakati ya Kwanza na ya pili hufanana sana na kitabu cha Waamuzi—mfano unarudiwa wa watu wanaompuuza Mungu, na wanapoangukia katika matatizo, wanamlilia Mungu, na kisha urejesho unafuatia. Vijana wana jina "Roller coaster," kwa hili likimaanisha "juu, chini, juu chini" Je, tunavunjaje mzunguko huu kwenda chini na kisha kwenda juu? Vijana wanahitaji mifano mizuri ya wazazi, ni kweli Manase alirudi kwenye zizi la Bwana ila kijana wake aliyeziona sanamu alibarikawaje?Upendo wa Mungu hauna masharti! Anampenda hata mkuu wa wakosaji, lakini anaichukia dhambi. Haijalishi dhambi zetu ni kubwa kiasi gani, Yeye Yuko tayari kutusamehe ikiwa sisi tutaitikia chanya kwa maagizo Yake, na adhabu tunazojipatia mara zingine ni matokeo ya asili ya dhambi zetu. Mungu wetu anamaanisha anachosema, "Sifurahii kufa kwake mtu mwovu, bali mtu mwovu aghairi njia yake na kuishi" (Ezekieli 33:11). Manase alisamehewa na kuokolewa, kwa sababu alijinyenyekeza na kutubu dhambi zake kweli kweli, hii inathibitisha kwamba Mungu anamaanisha kile anachokisema, "Haya, njoni, tusemezane, asema BWANA. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu." Isaya 1:18. Hakuna mtu, ambaye ni mwenye dhambi ambaye atashindwa kusamehewa ikiwa atatubu.

*"Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa," Kwa nini hatumwendei MUNGU kwa Neno Lake? Kuomba na kupokea vimeunganishwa kwa karibu. Ikiwa utaomba kwa imani mambo ambayo MUNGU ameahidi, utapokea. Mwangalie Yesu kwa ajili ya mambo unayohitaji. Mwombe msamaha wa dhambi, na unapoomba kwa imani moyo wako utalainishwa, na utawasamehe wale waliokuumiza, na maombi yako yatakwenda kwa MUNGU yakiwa na harufu nzuri ya upendo. Pamoja na kuomba huja kukesha katika maombi, na kila wazo na neno na tendo vitaambatana na ombi lako la dhati kwa ajili ya matengenezo katika maisha. Maombi ya imani huleta matunda stahiki. Lakini kutamka aina ya maneno tu kwa desturi, au mfano, bila unyofu wa dhati na matamanio ya dhati ya msaada, bila kutarajia utapokea, haitakufaa kitu. Mwombaji wa namna hii asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. Wale wanaokuja kwa MUNGU lazima waamini kwamba Yeye Yuko, na kwamba Yeye ni mtoa thawabu wa wale wanaomtafuta kwa bidii.

---

Manase alifanya uovu gani? Kwa nini alijirudi? Hilkia aliona kitabu cha namna gani? Shafani alikuwa na kazi gani? Kwa nini Yosia alilia? Nabii Hulda alimwambia nini Yosia? Kwa nini kiburi ni dhambi ngumu sana? Kwanini watu husema bahati ya mwenzako usilalie mlango wazi? Kwanini wazazi huumia wanapoona watoto wao wakifanya maamuzi mabaya.

**SIKU YA 145**
**(Mei 24)**

# Yosia Afanya Matengenezo

**- 2 Wafalme 23; Mambo ya Nyakati 34-35**



Mfalme akatuma wajumbe, na wazee wote wa Yerusalemu wazee wakaja. Mfalme akapanda nyumbani mwa BWANA, yaani hekaluni, na manabii na makuhani na watu wote wakubwa kwa wadogo, akasoma masikioni mwao kitabu cha agano kilichoonekana nyumbani mwa BWANA. Mfalme akafanya agano mbele za BWANA ili kumfuata, pia kuyashika maagizo Yake, shuhuda, na amri Zake kwa moyo wake na roho yake yote. Watu wote wakalikubali agano lile. Mfalme akaamuru makuhani kama Hilkia na walinzi waondoe vyombo vile wavyovitumia kwa ajili ya Baali na Ashera akavichoma moto nje ya Yerusalemu. Kisha akawafuta kazi makuhani waliofanya kazi ya kufukiza uvumba kwa miungu ya Baali, Ashera, jua, mwezi, sayari, nyota na sanamu za mbinguni. Akaiondoa Ashera katika nyumba ya Bwana akaichoma moto, na kuipondaponda iwe mavumbi, na kutupa mavumbi yake kwenye makaburi.

Akaziangusha nyumba za watu wasiofaa, waliokuwapo nyumbani mwa BWANA. Akapiga marufuku kupitisha watoto motoni, na kubomoa madhabahu hiyo. Akachoma moto magari ya jua ya ibada za uovu, na akatoa farasi waliohusika na ibada zile. Akaziteketeza madhabahu za miungu migeni walizofanya wafalme waliomtangulia. Alivunja madhabahu ile ya Betheli aliyoanzisha Yeroboamu mwana

wa Nebati. Aliona mifupa kwenye kaburi la yule mtu wa Mungu aliyeliwa na simba, hiyo alisema iachwe. Aliwaua wale makuhani wa uovu na kuteketeza mifupa yao kama Neno la BWANA lilivyokuwa limetabiri. Naye Akarudi Yerusalemu.

Kisa cha Mfalme Yosia kinarudiwa katika maisha ya Timotheo katika Agano Jipya. Wote wawili walibarikiwa kwa sababu ya mama na nyanya waliomcha Mungu. Sio kwa bahati mbaya kwamba mama na nyanya yake Yosia wametajwa katika maandishi tunayosoma leo: Jedida na Adaya. Je, unamkumbuka mama na nyanya ya Timotheo? Yunike na Loisi. Je, una mama au bibi/nyanya mcha Mungu aliyeyabariki maisha yako? Mshukuru BWANA leo, na kutoa ushuhuda wako! Daudi naye kama baba alimbariki mtoto wake Sulemani kwa maisha yake ya ucha Mungu. Hakika kuwa na wazazi wacha Mungu ni tunu kubwa, na pia kuwa na watoto wacha Mungu ni tunu kubwa zaidi! Hakuna matengenezo au uamsho bila Maandiko Matakatifu. "Kila mwanadamu mwenye akili ana uwezo wa kuchagua haki anapodai amri za Mungu. Katika kila uzoefu wa maisha, Neno la Mungu kwetu ni, 'Chagueni hivi leo nani mtakayemtumikia'.

Kijana anapotoa maisha yake kwa Mungu, anakuwa chombo chenye nguvu cha kufanya mema mikononi mwa Mungu kuliko hata mzee. Shetani anafahamu ukweli huu kwa hiyo amebuni njia nyingi za kuwanasa vijana wetu wachanga. Anaonekana kuwa na mafanikio fulani kwani vijana wengi hawako kanisani. Tunaweza kufanya nini kama washiriki basi? Wengine hufikiri muziki mdundiko na burudani zitawavutia, lakini hivi havijaleta wakristo makini! Tuendelee kuwaombea na kuwapenda bila masharti, yaweza kuwa ndiyo jambo litakaloleta tofauti. Kile ambacho hatuwezi kufanya, Mungu anaweza! 1 Yoh 2:13 Yasema hivi "Nawaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mmemjua Yeye aliye tangu mwanzo. Nawaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mmemshinda yule mwovu. Nimewaandikia ninyi, watoto, kwa sababu mmemjua Baba". Tudai ahadi hizi!

Mahali wakaapo washiriki pako chini ya Mimbari (the pulpit is above the pew), ikimaanisha kwamba endapo viongozi wa kiroho watasimamia mambo vyema hali ya kiroho ya nchi kwa kawaida inakuwa bora. Mfalme Yosia aliweka mfano kwa kuahidi hadharani kuzitii amri zote za Mungu kama Kitabu cha Sheria kilivyosema naye alikuwa mwaminifu kwa ahadi hiyo. Watu walifuata mfano wake, na kukawa na uamsho! Hebu wachungaji na waamke na kuongoza watu, maana mimbari daima ipo juu ya pale washiriki wanapokaa.

Aliendelea kuondoa wenye pepo wa utambuzi, wachawi, vinyago, na sanamu na machukizo yote yaliyoonekana katika nchi kuitimiza ile torati ya kitabu alichokipata Hilkia Kuhani. Hakuna mfalme mwingine aliyemwelekea BWANA kwa moyo wake, roho, na nguvu zake sawasawa na sheria ya Musa kama Yosia, wala baada yake hakuinuka mmoja mfano wake yeye. Yosia alijitahidi sana, lakini yale aliyofanya baba yake yalikuwa yameenda mbali sana, na adhabu ya kuchukuliwa utumwani Babeli ilikuwa inawangoja.

Basi Farao Neko, mfalme wa Misri akawekwa kupigana na mfalme wa Ashuru, naye akafika mto Frati, naye mfalme Yosia akaenda kupigana naye. Mungu

alimwagiza Farao Neko aende awapige Waashuru. Yosia alipoambiwa na Neko "acha kumpinga Mungu wako aliye pamoja nami asikuharibu," hakukubali. Basi Yosia akatoka kupigana na mfalme wa Misri, nao wapiga upinde wakampiga Yosia katika bonde la Megido. Watumishi wake wakamchukua garini wakamleta Yerusalemu; naye akafa, akazikwa makaburini mwa baba zake. Wakamwombolezea. Hakika Yosia angeyafuata maagizo ya Mungu asingeagamia vile. Ila sote tuna ukaidi mwingi na hivyo tumwombe Mungu tujisalimishe Kwake. Yuda wote. Watu wa nchi wakamtwaa Yehoahazi mwanawe wa umri wa miaka 23, wakamtawaza awe mfalme, naye alitawala miezi mitatu na kufanya maovu. Farao Neko akamfunga ili asitawale na kuitoza nchi kodi, na akamweka Eliakimu mwana mwingine wa Yosia ili atawale, akambadilisha jina lake kuwa Yehoyakimu. Huyu akampa Farao fedha, dhahabu akitoza watu ushuru. Yehoyakimu alikuwa na miaka 25 alipoanza kutawala, akatawala kwa miaka 11. Akafanya maovu machoni mwa BWANA.

Katika siku za Yehoyakimu, Nebukadreza mfalme wa Babeli akakwea kuchukua nchi,na mfalme Yehoyakimu akawa mtumwa wake kwa miaka mitatu, kisha akageuka akamwasi. Yehoyakimu alipolala mauti, mwanawe Yekonia akatawala mahali pake. Mfalme wa Misri hakuja Yerusalemu, ila Wakaldayo ndio walikuwa wana sauti ya kutawala nchi sasa. Yekonia alitawala miezi mitatu kwa uovu kama wafalme wengi waliopita. Wasaidizi wa mfalme Nebukadreza wa Babeli wakaja kuuhusuru Yerusalemu. Yekonia alitoka yeye, familia yake, mamaye, mashujaa, mafundi, watu wenye nguvu, watu wa koo za kifalme, watu matajiri, wafua chuma, maafisa na watumishi wake, na Nebukadreza akawachukua mateka watu elfu kumi, katika mwaka wa nane wa kutawala kwake. Walibaki watu wanyonge na maskini tu. Kisha akavichukua vyombo vya dhahabu hekaluni, vile ambavyo Sulemani aliweka na hazina za hekalu na nyumba ya mfalme. Mfalme Nebukadreza akamtawaza Matania, ndugu ya baba yake Yekonia awe mfalme badala yake, akabadili jina lake kuwa Sedekia.

Nebukadneza tukimwangalia juu juu tunaona kuwa ni mfalme mkatili, lakini tutaona baadaye kuwa alikuwa ni mwenye mawazo ya kina, mpanga mikakati mahiri, na mtawala mwenye heshima ambaye mara anapotambua thamani ya kweli ya mtu fulani au kitu fulani, yeye huonyesha kuzingatia ipasavyo. Ikumbukwe kwamba Nebukadneza hakuwahi kunajisi vyombo vya hekalu - alivitendea kwa heshima ya juu!. Na hatimaye alipopata kufahamu kuwa Mungu ni nani ... alimpa Mungu ibada ifaayo. Kisa hiki cha kustaajabisha ni sehemu ya mandhari ya kitabu cha ajabu cha kinabii cha Danieli. Kisa cha kusisimua sana ambacho unapaswa kukisoma tena na tena! Danieli 2 napoisoma huwa naona kama naruka juu na nipo kwenye ndege nikitizama chini mlima Kilimanjaro, Bonde la ufa, Serengeti, mto Naili, Bahari ya Hindi, Mto Kongo, Bahari ya Atlantiki, Jangwa la Sahara, Ziwa Viktoria na mambo mengine mazuri katika Jiografia ya dunia! Mungu huyo huyo wa neema angali anatenda kazi hata leo katika maisha yetu, kama alivyotenda katika maisha ya Danieli, Haleluya!

Wafalme wa Israeli Katika mpangilio wa nyakati za tawala zao, wao ni:
# Jina, miaka ya utawala, Mwisho wake na Matukio Mashuhuri ya Utawala wake

1. Sauli- Miaka 40 Aliuawa katika vita na Wafilisti, na kufuatiwa na Ishboshethi

Aliyetiwa Mafuta chini ya upinzani.

2. Ishboshethi Miaka 2 Aliuawa na waliokula njama, akapokelewa na Daudi ambaye Alitangazwa kuwa mfalme, lakini hakutiwa mafuta.
3. Daudi Miaka alitawala 40 akafa, akifuatiwa na Sulemani, naye Akalileta Sanduku la Agano Yerusalemu
4. Sulemani Miaka 40 akafa, akifuatiwa na Rehoboamu aliyetawala Yuda; Yeroboamu akawa mfalme wa Israeli wakati wa utawala wa Rehoboamu. Kujengwa Hekalu la kwanza
5. Yeroboamu wa Kwanza Miaka 22 akafa, na kufuatiwa na Nadabu Alichukua mamlaka katika vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyogawanya ufalme ulioungana. Yuda walihifadhi ukoo wa Daudi.
6. Nadabu akauawa baada ya miaka 2 na Baasha mwana wa Abiya, akatawala mahali pake
7. Baasha miaka 24 akafa, akafuatiwa na Ela
8. Ela Miaka 2, Aliuawa na Zimri, aliyetawala baada yake
9. Zimri siku 7 alijiua katika jumba lake la kifalme na moto; vita vifupi vya wenyewe kwa wenyewe vilianza kati ya nyumba ya Tibni na Omri, ambapo Tibni alikufa na Omri akawa mfalme.
10. Omri Miaka 12 akafa, akifuatiwa na mwanawe Ahabu Alianzisha Samaria kuwa jiji kuu la Israeli.
11. Ahabu akauawa vitani baada ya kutawala miaka 22, akafuatwa na mwanawe Ahazia
12. Ahazia akatawala Miaka 2 Maumivu mabaya, akafuatiwa na mwanawe Yoramu
13. Yoramu akatawala Miaka 12 Akauawa na Yehu, aliyefuata baada yake.
14. Yehu alitawala Miaka 28 naye akafa, akafuatiwa na Yehoahazi akawaua wote -yaani mfalme wa Israeli na mfalme wa Yuda.
15. Yehoahazi alitawala Miaka 17 akafa, akafuatiwa na Yehoashi
16. Yehoashi akatawala Miaka 16 naye akafa, akafuatiwa na Yeroboamu, mwana wa Yehoashi.
17. Yeroboamu II alitawala Miaka 41 naye akafa, akafuatiwa na Zakaria. Mtu wa mwisho wa "nyumba ya Yehu"
18. Zakaria alitawala miezi 6 naye aliuawa na Shalumu mwana wa Yabeshi, aliyetawala mahali pake
19. Shalumu alitawala miezi sita naye aliuawa na Menahemu mwana wa Gadi, aliyetawala mahali pake
20. Menahemu alitawala Miaka 10 akafa, akafuatiwa na Pekahia
21. Pekahia alitawala miaka 2 akauawa na Peka mwana wa Remalia, naye akatawala mahali pake
22. Peka alitawala miaka 20 akauawa na Hoshea mwana wa Ela, aliyetawala mahali pake
23. Hoshea alitawala miaka 9 naye Alitekwa na kupelekwa Ashuru
24. Biblia Fandom imeandika makadirio haya

*Waombeeni Wengine—Hebu na tujitahidi kutembea katika nuru kama Kristo alivyo katika nuru. Bwana aligeuza utumwa wa Ayubu alipoomba, si kwa ajili yake tu, bali kwa ajili ya wale waliokuwa wakimpinga. Wakati Alipohisi kutamani sana kwamba

roho zilizomkosea zipate kusaidiwa, yeye mwenyewe alipata msaada. Tuombe, sio kwa ajili yetu tu, bali kwa wale ambao wametuumiza, na wanaoendelea kutuumiza. Omba, omba, hasa katika akili yako. Usimpe Bwana pumziko; kwa maana masikio Yake yako wazi ili kusikia maombi yenye unyoofu, yasichoka na yenye kusihi, wakati nafsi inaponyenyekezwa/inapojidhili mbele Zake.

*Kuna wale wanaokuzunguka ambao wana huzuni, ambao wanahitaji maneno ya huruma, upendo, na laini, na maombi yetu ya unyenyekevu, yenye kuonyesha sikitiko.

---

Mfalme Yosia alikufa katika mazingira gani? Uovu una mshahara gani? Nani alitawala Yuda baada ya Yosia? Mfalme wa Yuda aliyechukuliwa mateka kwenda Babeli ni nani? Ni watu gani waliobakia Yerusalemu bila kuchukuliwa mateka?

**SIKU YA 146**
**(Mei 25)**

# Ufalme wa Mwisho wa Yuda

**- 2 Wafalme 24-25; 2 Mambo ya Nyakati 35; Isaya 45**



Sedekia alikuwa na umri wa miaka 21 alipoanza kutawala, akatawala miaka 11 Yerusalemu, naye akafanya yaliyo maovu mbele za BWANA na kuwa na shingo ngumu, akiwadhihaki wajumbe ambao Mungu aliwatuma kwao. Sedekia ndiye alikuwa mfalme wa mwisho wa Yuda, kabla ya uhamisho wa mara ya tatu na wa mwisho kwenda Babeli. Japo Yeremia nabii alimwambia afanye vile ambavyo mfalme wa Babeli alikuwa amemwagiza, lakini Sedekia hakupokea ushauri wa nabii. Hata hakuwa tayari kumlinda Yeremia asidhurike. Sedekia akamwasi mfalme wa Babeli, naye Nebukadreza akaja yeye na jeshi lake lote kupigana na Yerusalemu, akapanga hema zake kuukabili, nao wakajenga ngome pande zote. Mji ukazingirwa na njaa ilikuwa nzito ndani ya mji. Ndipo mahali fulani pakabomolewa katika ukuta wa mji. Watu wote wa vita wakakimbia usiku kwa njia ya lango lililokuwa katika bustani ya mfalme. Wakaldayo walikuwa wakilinda mji pande zote, wakamfuata mfalme, na kumpata katika nchi tambarare ya Yeriko, na jeshi lake lote limetawanyika na kumwacha. Wakamkamata Sedekia, na kwenda kwa Nebukadreza, wakaua watoto wake mbele yake, kisha wakampofusha macho, na kumfunga pingu, wakamchukua mpaka Babeli. Kisha Nebukadreza alirudi na kuiteketeza nyumba ya BWANA, nyumba ya mfalme na nyumba za watu.

Wakazibomoa kuta za Yerusalemu pande zote na mabaki yote ya wale waliosalia katika mji, na wale walioasi, akaacha watunza mizabibu, maskini na wakulima tu. Walichukua vyombo vya shaba kama vile, masufuria, majembe, mikasi,

miiko, vyetezo, na mabakuli ya dhahabu na fedha. Wakachukua na nguzo za shaba na mapambo ya makomamanga. Kuhani mkuu Seraya na msaidizi wake Sefania wakachukuliwa. Akamchukua towashi mmoja ili asimamie wale waliobaki. Nebuzaradani ndiye aliyekuwa jemedari wa Babeli akifanya kazi hiyo. Akamweka Gedalia kuwa liwali juu ya wale waliobaki. Watu wakamwendea Gedalia kumwambia hofu zao, naye akawaambia, wasihofu, wamtumikie tu mfalme wa Babeli na itakuwa vyema kwao. Hili hawakulipenda, basi Ishmaeli na wana wa kifalme walimwendea Gedalia wakampiga na kumwua, na kukimbilia Misri wakiogopa Wakaldayo.

Ikawa mwaka wa thelathini na saba wa kuhamishwa Yekonia mfalme wa Yuda kwenda Babeli, Evil-merodaki mfalme wa Babeli katika mwaka wa kwanza wa kutawala kwake, akamtoa Yekonia gerezani, akasema naye maneno mazuri, na kumweka kwenye kiti chake cha enzi cha wafalme waliokuwa naye Babeli. Akambadilishia mavazi yake ya kifungwa, akala chakula mbele yake daima, siku zote za maisha yake, alipewa posho na mfalme. Bila shaka ukorofi wake wa kutosikiliza manabii ulimtoka kabisa.

Basi watu walioenda utumwani waliwatumikia wafalme wa Babeli na wana wao hata kulipoingia milki ya Uajemi, ili kulitimiza Neno la Bwana kwa kinywa cha Yeremia nabii, kwamba, hata nchi itakapofurahia Sabato Zake, kwa maana siku zote ilipokaa ukiwa ilishika Sabato, kutimiza miaka sabini. Wazazi wanapokosa kuwalea watoto wao katika njia ya Bwana, wanamweka mtoto katika hatari ya kupata majanga. Kwa kila mbegu ambayo wazazi hupanda katika maisha ya watoto wao, bila shaka watavuna. Pia viongozi wanaposhindwa kufanya yaliyo mema wanaruhusu jamii yao kunyang'anywa vitu bora walivyo navyo na kuachwa ukiwa. Mateso mengine huja kwa hekima ya Mungu ili kutuleta karibu na kiti cha neema. Yeye huwalainisha na kuwatiisha watoto Wake kwa huzuni na majaribu. Ulimwengu huu ni karakana ya Mungu, ambapo Yeye hutuunda kwa nyua za mbinguni. Anatumia kisu cha kupogoa mioyo yetu inayomangamanga hadi ukali na kasoro zake ziondolewe na tuwekwe mahali petu panapofaa katika jengo la mbinguni. Kupitia dhiki na fadhaa Mkristo anasafishwa na kuimarishwa ili akuze tabia kulingana na kielelezo ambacho Kristo ametoa. Mara nyingi adhabu Mungu anazozitoa, ni kwa wachache ili wengi wapone kwa kutopitia njia hiyo. Visa vya Uza, Kora na vinginevyo ni mfano.

Na sisi kama wazazi na viongozi tuwafundishe watoto wetu katika njia ya Bwana na tuchague kufanya yaliyo sawa machoni pa Mungu ili mambo yawe mazuri kwa familia zetu na jamii zetu.

Na katika mwaka wa kwanza wa Koreshi, mfalme wa Uajemi, Neno la
BWANA kupitia kwa nabii Yeremia lilitimizwa. Bwana akamwamsha roho yake Koreshi, akapiga mbiu katika ufalme wake wote, akaandika pia akisema, "Koreshi, mfalme wa Uajemi asema hivi, BWANA Mungu wa mbinguni amenipa falme zote za dunia; Naye ameniagiza nimjengee nyumba katika Yerusalemu, ulioko Yuda. Basi kila mtu katika ninyi nyote, mlio watu Wake BWANA Mungu wake, na awe pamoja naye, na akwee."

Mfalme Koreshi wa Uajemi, alikuwa mtumishi wa BWANA aliyetabiriwa kuzaliwa

kwake kabla ya miaka 150. Mungu alimwandaa ili kusaidia ujenzi wa hekalu, kusaidia watu Wake, kutiisha mataifa mbele yake, na kusawazisha palipokwaruzika. Alitoa mali kwa ajili ya shughuli zote, iwe ni dhahabu, miti, farasi, au punda. Koreshi alikuwa Mwajemi, lakini alimjua BWANA, kuwa ndiye mmoja, na hapana mwingine zaidi yake na akamtumikia kwa kicho. Jaribu kusoma kisa cha Koreshi alipokuwa mtoto. Ni kisa cha ajabu jinsi alivyochukuliwa na kulelewa na wazazi ambao hawakuwa na mtoto, na ilikuwa auawe akiwa mtoto, lakini alinusurika.

MAJINA YA WATAWALA WA YUDA, na tabia yao (wazao wote wa Daudi isipokuwa mtawala haramu # 7) TAREHE YA UTAWALA . MZURI AU MBAYA. MIAKA YA UTAWALA.
(kulingana na hesabu za kisasa)
1. Mfalme Rehoboamu 930-913 KK. Mbaya. 17. mwana wa Sulemani;
mama = Naama Mwamoni 1 Wafalme 11:42 – 14:31;
2 Mambo ya Nyakati 9:31-12:16

2. Mfalme Abiya (Abiya) 913-911 KK. Mbaya. 3 . mwana wa Rehoboamu; mama: Maaka (Mikaya), mzao wa Absalomu mwana wa Daudi 1 Wafalme 14:31 – 15:8;
2 Mambo ya Nyakati 13:1-23

3. Mfalme Asa 911-870 KK .Mwema. 41. mwana wa Abiya; mama?, Gebira = bibi Maaka 1 Wafalme 15:8-24;
2 Mambo ya Nyakati 13:23-16:14

4. Mfalme Yehoshafati 870-848 KK. Mwema. 25 . mwana wa Asa; mama: Azuba 1 Wafalme 15:24; 22:41-51;
2 Mambo ya Nyakati 17:1-21:1

5.Mfalme Yehoramu 848-841 KK. Mbaya. 8 . mwana wa Yehoshafati; mama:?
2 Wafalme 8:16-24;
2 Mambo ya Nyakati 21:1-20

6. Mfalme Ahazia 841- BC. Mbaya. 1 . mwana wa Yehoramu; mama: Athalia binti Yezebeli na Ahabu, Mfalme wa Ufalme wa Kaskazini wa Israeli 2 Wafalme 8:24-29; 9:14-26;
2 Mambo ya Nyakati 22:1-12

7. Malkia, Mama Athalia, Mbaya. 7 isiyo halali.
(mzao wa nasaba ya Omni wa Israeli) 841-835 KK. Binti wa Yezebeli na Ahabu, Mfalme wa Ufalme wa Kaskazini wa Israeli 2 Wafalme 8:26; 11:1-20;
2 Mambo ya Nyakati 21:6; 22:2, 22:9-23:21

8. Yehoashi (Yoashi) 835-796 KK,. Mwema. 40 . mjukuu wa Athalia na mwana wa Ahazia; mama: Zibia wa Beer-sheba 2 Wafalme 11:1 – 12:21;
2 Mambo ya Nyakati 22:10-23; 24:27

9. Amazia 796-781 KK. Mwema. 29. mwana wa Yehoashi; mama: Yehoadani wa

Yerusalemu 2 Wafalme 14:1-22;
2 Mambo ya Nyakati 24:27-25:28

10. Uzia 781-740 KK Alianza vizuri baadaye akawa mbaya. 52 . mwana wa Amazia mama: Yekolia wa Yerusalemu 2 Wafalme 15:1-7;
2 Mambo ya Nyakati 26:1-23

11. Yothamu (alihudumu kama mtawala kwa miaka kadhaa hadi kifo cha baba yake) 740-736 KK Mzuri. 16 . mwana wa Uzia; mama: Yerusha binti Sadoki 2 Wafalme 15:32-38;
2 Mambo ya Nyakati 26:21-23 ( regent );
26:23-27:9 (mfalme)

12. Ahazi 736-716 KK. Mbaya. 16 .mwana wa Yothamu; mama:? 2 Wafalme 15:38 – 16:20;
2 Mambo ya Nyakati 27:9-28:27

13. Hezekia 716-687 KK Mwema. 29 .mwana wa Ahazi; mama: Abiya binti Zekaria 2 Wafalme 16:20; 18:1- 20:21;
2 Mambo ya Nyakati 28:27-32:33

14. Manase 697-642 KK. Mbaya. 55 . mwana wa Hezekia; mama: Hebisiba 2 Wafalme 21:1-18;
2 Mambo ya Nyakati 32:33-33:20

15. Amoni 642-640 KK Mbaya. 2 . mwana wa Manase; mama: Meshulemethi binti Haruzi wa Yotba 2 Wafalme 21:18-26;
2 Mambo ya Nyakati 33:20-25

16. Yosia 640-609 KK Mwema 31 mwana wa Amoni; mama: Yedidia binti Adaya wa Bozkathi 2 Wafalme 21:26 – 23:30;
2 Mambo ya Nyakati 33:25-35:27

17. Yehoahazi 609 KK Mwovu mwana wa Yosia wa miezi 3;
mama: Hamutal
binti Yeremia wa Libna 2 Wafalme 23:30-34;
2 Mambo ya Nyakati 36:1-4

18. Yehoyakimu
(jina lilibadilishwa kutoka Eliakimu hadi Yehoyakimu na Neko, Farao wa Misri; labda linaonyesha hadhi ya kibaraka) 609-598 KK Mbaya 11 Mwana wa Yosia; ndugu ya Eliakimu/Yehoahazi;
mama: Zebida binti Pedaya wa Ruma 2 Wafalme 23:34 – 24:6;
2 Mambo ya Nyakati 36:5-8

19. Yehoyakini
(pia anajulikana kama Konia; aliitwa Yekonia katika N.T.) 598-597. KK . Mwana

wa Yehoyakimu. miezi 3. mbaya; mama: Nehusta binti Elnathani wa Yerusalemu 2 Wafalme 24:6-17
2 Mambo ya Nyakati 36:8-10

20. Sedekia (jina lililobadilishwa na kuwa Sedekia na Mfalme Nebukadneza wa Babeli labda linaonyesha hadhi ya kibaraka) 597-586 KK. Mbaya. 11 . mwana wa Yosia;
baba mdogo wa Yehohakini; mama: Hamitali binti Yeremia wa Libna (pia mama yake Mfalme Yehoahazi) 2 Wafalme 24:17 – 25:30
2 Mambo ya Nyakati 36:10-13;
Yeremia 52:1-3; 37-39;
Ezekieli 17:13-16...............

21. Yesu wa Nazareti, mwana wa Daudi, mwana wa Mungu 30AD- Milele. Umilele Usio na Dhambi. Mwana wa Mungu, mama: Maria wa Nazareti, mzao wa Mfalme Daudi: Mathayo 1:1-17, 20; Luka 1:26-38; 2:5; 3:23-38; Ufunuo 12:1-17
Tarehe zote ni za makadirio na zinaweza kutofautiana kulingana na wasomi mbalimbali
Huduma ya Agape


*Tunapotafuta kuwaleta wengine kwa Kristo, tukibeba mzigo wa roho katika maombi yetu, mioyo yetu itapatwa na ushawishi wa kuhuisha wa neema ya MUNGU; mapenzi yetu yatang'aa  zaidi kwa jitihada za Bwana; maisha yetu yote ya Kikristo yatakuwa ya kweli na halisi zaidi, yenye bidii zaidi, na ya maombi zaidi.

---

Gedalia alikuwa nani? Evil-Merodaki alimfanyiaje Yekonia? Sedekia alipata adhabu gani kwa kutosikia? Ni kwa vipi Koreshi alikuwa mtumishi wa Mungu?

**SIKU YA 147**
**(Mei 26)**

# Ezra – Kuhani aliuelekeza moyo wake kuitafuta sheria ya Bwana na kuitenda!




Ezra alikuwa ni kuhani na mwandishi wa Sheria ya Musa. Kitabu cha Ezra ni cha Historia na majina ya ukoo. Kitabu hiki kiliandikwa takribani 450KK. Watu wahusika ni mfalme Koreshi, kuhani Ezra, nabii Hagai, nabii Zekaria, mfalme Dario, mfalme Ahasuero, na kiongozi Zerubabeli. Kwenye Maandiko ya Yeremia na Isaya, Mungu aliwaahidi watu Wake kwamba watarudi kutoka uhamishoni Babeli baada ya miaka 70. Koreshi alikuwa chombo ambacho Mungu alikitumia katika kurudi kwao. Isaya 45:1 na 44:28. Familia za watu kabila la Yuda na Benjamini, makuhani na walawi, na wale ambao Mungu aliwasukuma walitoka kwenda kumjengea Mungu nyumba Yake, ukuta na pia kurudisha huduma za kiroho. Ezra 1:5 yaonyesha Ezra alikubali kwenda, alikuwa kiongozi na na mwalimu wa Maandiko. Fungu hili lina maana nzito ambayo inatubidisha nasi kufanya vile "Kwa maana huyo Ezra alikuwa ameuelekeza moyo wake kuitafuta sheria ya Bwana, na kuitenda, na kufundisha maagizo na hukumu katika Israeli" 7:10. Zerubabeli aliitikia wito wa Bwana na kwenda takribani 538 KK kujenga hekalu na Ezra 457 KK kusaidia

umsho kwa Maandiko na Nehemia 444 KK kusaidia kujenga ukuta. Ezra aliitwa kwenye utumishi mwaka ule mfalme Ahusuero alipotoa tangazo la kukarabatiwa kwa Yerusalemu na hili tangazo linahusiana na Daniel 9:24-27. Soma zaidi unabii huu wa siku 2300 kwenye kitabu cha Danieli 8 na 9. Maneno yaliyoandikwa kwenye kitabu cha Ezra yanajibu maswali ya vipande vilivyokosekana katika kitabu cha Daniel, yaani historia ya unabii ya huduma ya Kristo, na kazi Yake Kwa niaba yetu. Miaka ile 70 ambayo ilianza mwaka ule wa 457 BC, miaka ile 490, mwaka ule wa 34BK, na zile siku 2300 (miaka 2300) na ile miaka 490, miaka 1810, na hata ule mwaka wa 1844. Ezra, Zerubabeli na Nehemia walishugulikia mambo ya uamsho na matengenezo kwa wale waliorudi kwenye nyanja

Baada ya uhamisho kwenda utumwani, mateka waliruhusiwa kurudi wakati Wamedi na Waajemi wanatawala chini ya mfalme Koreshi. Zerubabeli alirudi kwanza na watu 50,000 kujenga hekalu jipya. Walipanga na kutafuta vifaa na kuanza kujenga ila walijenga polepole kwa vile walikuwa na maadui wanaowaogopesha. Wakasimamisha kazi miaka miwili, lakini baada ya miaka ishirini walimaliza. Wakafanya sikukuu ya Pasaka na kujitakasa kwa siku saba, kisha wakaweka wakfu hekalu.

Watu kama Danieli au Ezekieli na wengine waliokuwa wazee, au walioridhika kuishi ugenini hawakurudi, bali waliendelea kukaa Babeli. Kitabu cha Ezra na Nehemia hakimaliziki kwa matumaini. Dhambi ni jambo zito, linaloenea kwa urahisi na haraka. Changamoto kubwa haitoki nje kwa makafiri, bali bali kwa watu waliomjua Mungu na kisha wasiyafuate mapenzi yake yaliyofunuliwa fika. Kuwa mwaminifu kwa Bwana na kudumu katika kufuata maagizo Yake ni mtihani mkubwa sana kwa kanisa la Mungu. Kama Ezra alivyoelewa kwa usahihi, nguvu pekee ya mabadiliko huja kwa kuyachunguza Maandiko kwa bidii, kuyaelewa, na kuyaweka ndani. Ili kutimiza sehemu ya kuanzia ya unabii wa yale majuma 70 na jioni na asubuhi 2,300 (ambayo yote yalianza mwaka wa 457 KK.), Mungu aliingilia kati kwa neema na kumshawishi Mfalme Artashasta wa Kwanza amruhusu Ezra pamoja na kundi la Waisraeli kurudi Yerusalemu. Ili kupata usalama wa safari yao, na hata kutoa mahitaji ya kimwili na ya kifedha yanayohitajika kwa ajili ya huduma za hekalu ( Ezra 7:11-28 ). Mada kuu za vitabu hivi viwili ni majaliwa ya Mungu, uaminifu, na Agano Lake. Mungu alitimiza ahadi Zake, ingawa watu Wake walikuwa na mawazo finyu, waliochanganyikiwa, waliokengeushwa, na wakaidi. Kupitia kwa watumishi Wake, Aliwaita kutoka katika hali yao ya ulegevu hadi kwenye uamsho na matengenezo.

Ezra alisukumwa na Roho Mtakatifu, na akawa ushawishi wenye msukumo kwa watoto na wazee vile vile. Wengi katika Yerusalemu walikuwa wamerudi kutoka uhamishoni wakiwa tayari kumtii Mungu hata kuacha mahusiano yao ya kipagani. Mkono wa Ezra ulitiwa nguvu na watu hawa. Aliinuka kwenye mvua kubwa na kuanza kusoma majina ya wale waliokuwa na shida ya ndoa za kipagani.
Yesu Kristo Muumba wetu, Mwokozi, na kiongozi mkuu kuliko wote, alijinyenyekeza mbele ya ulimwengu unaotazama. Alitoa maisha yake kama dhabihu kuu kwa vizazi vyote vya watu na kwa umilele wote. Kwa hiyo, hata tukiwa wadhambi na dhaifu, tunaweza kuwa na nguvu kupitia tumaini na imani yetu Kwake. Jibu langu ni, Yesu,

nina nguvu pamoja Nawe, ninakufuata na nitaishi nikikuamini Wewe, hata katika kukabiliana na upinzani.

Nasaba zimetajwa kwenye kitabu hiki zikitukumbusha kuwa hii ni historia ya kweli, na ahadi za Mungu hutimia, na hivyo Mungu ni Mwaminifu. Yawezekana wengi waliacha marafiki zao kule Babeli na wakawakumbuka, ila mara zingine katika maisha lazima tuwe tayari kuwaacha marafiki, ndugu na jamaa, kama hawataki kuambatana nasi, ili tuweze kufanya mambo makubwa zaidi kwetu wenyewe na kwa utukufu wa Mungu. Tukisoma hii orodha Swali hili linanijia!
JE! JINA LANGU LIMEANDIKWA HAPO? Swali ni kwako na kwangu!
Mara nyingi tunashangaa kwa nini orodha ndefu za majina zimeandikwa katika Biblia.

Jibu ni rahisi: hii ni historia. Ni ushuhuda wa chaguzi ambazo zimefanywa. Ni uhakikisho wa unabii, hakika Mungu anamjua kila mmoja wetu na ana shauku naye kama mwandishi wa Zaburi alivyosema kuhusu rekodi zetu, na hata za mahali tulikozaliwa ni vipengele vidogo ila muhimu kwa Mungu kwani "Bwana atahesabu, atakapoandika watu, kwamba mtu huyu alizaliwa hapo" Zaburi 87:6. Yaani atakaponihesabu mimi, atasema "Huyu alizaliwa Bariadi, Tanzania!" Hii inanipa moyo kwamba Mungu anapenda habari zetu zote kwa kinagaubaga na hata vipengele vidogo zaidi kunihusu mimi, kuliko mimi mwenyewe kwa umbali mno! Hakika mambo mengine Mungu atatuelezea zaidi tukifika mbinguni!
Kuna orodha ya majina katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.
Ninashukuru sana kuwa jina langu na lako limeandikwa humo, tangu tulipomwamini Yesu kama Mwokozi na Bwana wetu binafsi! Unasemaje huko rafiki msomaji?

*Kuna nafsi ambazo zimepoteza ujasiri wao; zungumza nao, uwaombee. Kuna wanaohitaji Mkate wa Uzima. Wasomee kutoka katika Neno la MUNGU. Kuna ugonjwa wa roho ambao hakuna zeri inayoweza kuugusa, hakuna dawa inayoweza kuponya. Waombee hawa, na uwalete kwa Yesu Kristo. Na katika kazi yako yote Kristo atakuwepo kufanya ushawishi kwenye mioyo ya wanadamu.

---

Elezea Kuhusu nyadhifa za Ezra, Zerubabeli na Nehemia

**SIKU YA 148**
**(Mei 27)**

# Ezra na Nehemia wana Uamsho na Matengenezo

Kitabu cha Nehemia ni cha kihistoria. Kiliandikwa na Ezra na Nehemia wenyewe. Wengi husema Ezra alihusika zaidi, na vitabu hivi vilikuwa kimoja vikatenganishwa. Wahusika ni mnyweshaji Nehemia, kuhani Ezra, Sanbalati na Tobia. Yerusalemu ilikuwa na hekalu lakini hapakuwa na ukuta wa kusaidia usalama. Walichukua siku 52 kujenga kuta. Nehemia anasema, "Ndipo maadui zetu waliposikia, ndipo makafiri wote waliotuzunguka, wakaogopa nao wakakata tamaa sana machoni pao wenyewe, maana waliitambua kazi hiyo ilivyotendwa na Mungu wetu." Katika mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake mfalme Koreshi wa Uajemi, neno la BWANA alilolitoa kupitia nabii Yeremia lilitimia. Koreshi alipiga mbiu katika ufalme wake wote kwamba Mungu amemwagiza amjengee nyumba Yake katika Yerusalemu ulioko Yuda. Koreshi akaruhusu watu warudi na kujenga nyumba ya BWANA na yeye atawasaidia vifaa na mali. Basi alisaidia watu hata usafiri ili waweze kufanya safari hiyo. Koreshi akavitoa vyombo vya nyumba ya BWANA alivyoleta Nebukadreza ili wavipeleke kupitia mtunza hazina, nao wakavihesabu. Sheshabaza akakwea navyo. Wakaenda na Zerubabeli kama watu 50,000 hivi. Walipofika Yerusalemu, watu walitoa kwa ukarimu kwa ajili ya nyumba ya Mungu ili kuisimamisha. Watu wengine wakitaka kupoteza lengo, walijidai kuja kusaidia lakini kuhani Zerubabeli na Yoshua waliwaambia, "ninyi msishirikiane nasi, tutafanya peke yetu, haiwahusu, kama mfalme Koreshi wa Uajemi alivyoamuru." Watu hawa waliajiri watu kuwapinga kama Tatenai, lakini Mungu akawasaidia wakamaliza. Walipomaliza walimhimidi BWANA na kuimba kwa baragumu na matoazi, wakimshukuru BWANA. Lakini wale waliokumbuka jinsi hekalu lililojengwa na Sulemani lilivyokuwa la fahari kubwa, walilia machozi, japo na kelele za furaha pia zilikuwa nyingi.

Jambo jingine tunaliona ni kwamba wazee walikuwa wameuona utukufu wa hekalu la Sulemani, nao wakaomboleza kwa sababu ya hali duni ya jengo ambalo sasa lingejengwa, Nehemia aliomba ruhusa kwa mfalme, kisha akarudi tena kazini kwake kama mnyweshaji wa mfalme, akaomba ruhusa tena na kurudi mara ya pili. Nehemia alisikitika sana aliposikia hali ya Yerusalemu.

Ezra aliongoza watu kusherehekea kujitoa upya kwa BWANA. Hii ni pamoja na kufundisha sheria na kuzielezea kwa watu. Walijua kuwa ikiwa wanataka wapone kama taifa, ni lazima wazingatie kutii sheria. Na watu wakakusanyika kama mtu mmoja katika uwanja uliokuwa mbele ya lango la mji, Ezra mwandishi akaleta kitabu cha Torati ya Musa, BWANA aliyowaamuru Waisraeli, naye akaisoma mbele ya wote walioweza kusikia na kufahamu.

Nehemia aliwarudisha Walawi na kuwapa posho, ili waendelee kuhudumu hekaluni.

Akaweka watu kila mtu na kazi yake, iwe ni kulinda au kuleta kuni. Nehemia alisihi akisema, "Unikumbukie hayo nayo, Ee Mungu wangu, wala usifute fadhili zangu nilizozitenda kwa ajili ya nyumba ya Mungu wangu, na kwa taratibu zake."

Nehemia aliona watu wakisindika zabibu na kufanya kazi siku ya Sabato, na wengine wanachukua mazao shambani na kuwabebesha punda wao. Walileta mizigo ya aina zote Yerusalemu, iwe ni matunda, samaki, nk. siku ya Sabato na kuwauzia wana wa Yuda. Nehemia akaenda kuwaambia wakuu, "Ni neno baya gani hili mnalofanya ninyi, na kuinajisi siku ya Sabato?" Uvunjaji wa amri za Mungu ndio uliofanya baba zao wakachukuliwa mateka kwenda utumwani. Nehemia akaamuru kuwa kabla ya jua kutua na Sabato kuanza, mlango ifungwe na isifunguliwe mpaka Sabato iishe, na bidhaa za uchuuzi zisiingie. Kisha akaona wengine wanalala na mizigo nje ya ukuta, wakingoja Sabato iishe ili waendelee na uchuuzi. Tunapaswa tulinde pindo za Sabato, saa chache kabla ya jua kutua Ijumaa, na saa chache kabla ya jua kutua Jumamosi! Ni rahisi kupitiliza na kuendelea na kazi zetu katika masaa matakatifu. Nehemia akawaambia kuwa atawakamata, basi walipata woga na hawakurudi tena! Nehemia akawaambia Walawi wajitakase na kulinda malango ili kuitakasa siku ya Sabato. Matengenezo ya mihimili mikuu ya mafundisho ya imani yalishugulikiwa na Mashujaa hawa wawili wa imani, Ezra na Nehemia.

Nehemia akaona Wayahudi waliokuwa wameoa wanawake wageni wa Ashdodi, na Amoni na Moabu, watoto wao pia walishindwa kuongea Kiyahudi. Nehemia aliwapiga baadhi yao na kuwanyoa nywele zao, akawaapisha watu wasioane na wa-Mataifa wasiomcha Mungu. "Je! Sulemani, mwana wa Daudi, hakufanya dhambi kwa kutenda hayo? Japo alipendwa na alikuwa na hekima, lakini wanawake wageni walimkosesha hata yeye. Nehemia akasema wasitende uovu huu, na kumhalifu Mungu kwa kuoa wanawake wageni. Nehemia akamfukuza kuhani aliyeoa mwanamke mgeni. Ezra na Nehemia walisimamia watu kwa hili hata kurarua nguo zao, na kuutafuta uso wa BWANA katika hili. Ezra aling'oa nywele za kichwa chake na ndevu zake na kuketi kwa mshangao. Hata leo tuna hatari ya kuwa na urafiki wa karibu na wale wasiomjali Mungu, na hata kufungiwa nira nao; tunajiingiza katika hatari kubwa. Nehemia aliomba kwa Mungu kwa ajili ya watu Wake waliooa wanawake wageni. Watu wakaja karibu na Ezra aliyekuwa akiungama na kulia. Basi wakafanya agano na Mungu la kuachana na wake zao wageni wakitaka mambo haya yatendeke kwa kuifuata torati. Akawaambia waungame, ili wasiongeze hatia katika Israeli.

Maombi ya Nehemia yalikuwa na kusudi imara—Kuna hitaji la akina Nehemia katika kanisa leo,—sio watu wanaoweza kuomba na kuhubiri tu, bali watu ambao maombi na mahubiri yao yameimarishwa kwa kusudi thabiti, ari/usongo na matamanio makubwa. Hebu fikiria basi, kwamba Mungu Mwenye hekima na uwezo wote hakuwa na njia yoyote ya kutuokoa isipokuwa kuja duniani na kupata mateso na fadhaa , Naye akaja, basi tujue kwamba pambano hilo kati ya wema na uovu ni kali sana. Na Kwamba Yesu anatupenda mno, kuliko tunavyofikiria. Yaani anatupenda Mno kuliko Anavyojipenda na tunavyojipenda Mwenyewe! Nafikiri hitimisho hili walikuja nalo kwanza malaika wa mbinguni! Hapo mwanzo wengine walijitenga na kumfuata Shetani, ila wale waliobakia hawakuwa na uhakika kuwa

Mungu hakika alivipenda viumbe Vyake kiasi kile. Ila walipoona Yesu anateswa na kudhalilisha na Mungu hafanyi kitu, pengine walimwambia fanya kitu Bwana wetu asife au asipate fadhaa kiasi hiki, ila walipoona Yesu anafedheheshwa, anaumizwa na kisha kuuwawa, walipata mshtuko na mshangao papo hapo. Pengine hata walisema mioyoni mwao "Huyu Mungu jamani! Sisi tuko hoi, kwamba kwamba anawapenda hawa viumbe na pia sisi kiasi hiki? Kwamba anawapenda hawa binadamu kupita anavyojipenda Mwenyewe?" Hakika ni kitendawili kitakachosimuliwa milele zote na utamu na urojororojo wake usiishe milele zote! Yaani baada ya machafuko kuletwa na shetani,  sayari zote na himaya yote ya Mungu ilikuwa hatarini mno, ila katika Hekima Yake Mungu, machafuko haya yameweza kutatuliwa, mara moja na milele zote. Hakuna ambaye anaweza kukataa au kupinga kwamba Mungu anatupenda kuliko anavyojipenda Mwenyewe!

*Hebu wale walio wa kiroho wazungumze na nafsi hizi. Omba nao na kwa ajili yao. Hebu muda mwingi utumike katika maombi na kulichunguza Neno kwa karibu. Hebu wote wapate mambo ya halisi na ya  kweli ya imani katika nafsi zao wenyewe kwa njia ya imani kwamba Roho Mtakatifu atakabidhiwa kwao kwa sababu wana njaa na kiu ya Kweli ya haki.

---


Nehemia alishugulikiaje wale waliofanya biashara siku ya Sabato? Kwa nini Ezra aling'oa ndevu zake? Sulemani alifanya dhambi gani? Zerubabeli alirudi na watu wangapi Yerusalemu? Je, leo kanisani kwako kiongozi akiwapiga watu na kuwanyoa nywele zao ili wafanye matengenezo ya kiroho, watamchukuliaje?

**SIKU YA 149**
**(Mei 28)**

# Nehemia – Rafiki ya Mfalme Asema MUNGU Wetu Atatupigania

Akiwa ni mnyweshaji wa mfalme wa Uajemi, Nehemia aliwauliza watu waliotoka Yuda kuhusu hali ya mambo ilivyokuwa huko Yerusalemu. Ilikuwa imepita miaka 90 toka watu wa kwanza wa uhamisho warudi Uyahudi. Wakamwambia kuwa kuna dhiki nyingi na mashutumu, kwani ukuta wa Yerusalemu umebomolewa na malango yake yameteketezwa kwa moto. Nehemia aliketi, akalia na kuomboleza siku kadha wa kadha, kisha akafunga. Hakika Maombi ni siri kubwa ya ushindi. Akamsihi Mungu asikilize maombi yake kwa ajili ya watu wake Israeli, akasema, "Tumefanya dhambi, tumetenda maovu mengi juu yako, wala hatukuzishika amri wala sheria wala hukumu ulizomwamuru Musa mtumishi wako." Akamwomba BWANA atege sikio Lake kwa watumishi Wake wanaomcha na kuwafanikisha. Nehemia alikuwa mnyweshaji wa mfalme, kazi ya hatari kwani ndiye aliyeonja vinywaji vya mfalme kabla ya mfalme ili kama vina sumu mfalme asidhurike. Mfalme Artashasta ndiye alikuwa akitawala basi alishika divai ampe, naye siku za nyuma hakuwa na huzuni, isipokuwa baada ya kusikia habari za Yerusalemu. Ni hatari kukasirika mbele ya mfalme, maana unaweza kuonekana una njama fulani. Mfalme alimwuliza Nehemia kwa nini ana huzuni, je, ana ugonjwa? Nehemia akasema haumwi ila ana huzuni ya moyo. Akamwambia mfalme, "Mfalme na aishi milele; kwani uso wangu usiwe na huzuni, iwapo mji, ulio mahali pa makaburi ya baba zangu unakaa, unakaa ukiwa na malango yake yameteketezwa kwa moto?" Mfalme akamwambia amsaidie nini? Naye akasema kama amepata kibali mbele zako "tafadhali unipeleke mpaka Yuda, niuendee mji wa makaburi ya baba zangu, nipate kuujenga." Mfalme akamwuliza mbele ya malkia, "safari yako itakuwa ya siku ngapi?" Nehemia akampa muda, akaomba na barua ya utambulisho na mamlaka ya kuwapa viongozi kule Uyahudi ili afanye shughuli hiyo. Akapewa waraka wa kupata miti, na mengineyo. Naye anasema, "Naye mfalme akanipa, kama mkono mwema wa Mungu wangu ulivyokuwa juu yangu."

Basi akafika kwa wale maliwali waliokuwa ng'ambo ya Mto. Kazi ya ujenzi ikaendelea. Lakini Sanbalati na Tobia, Mwamoni, waliposikia kwamba ujenzi unaendelea, wakahuzunika, maana walitaka kupinga kazi ya BWANA. Hawa walipata uchungu, na kunena kwa kebehi juu ya kazi ile. Tobia akasema, "hiki wanachokijenga, angepanda mbweha angeubomoa ukuta wao wa mawe." Nehemia akaendelea kumwomba Mungu. Aliondoka usiku ili kukagua kazi kwani hakutaka kuwapa watu nafasi ya kupinga kazi iliyokuwa inafanyika. Walijenga, lakini ilibidi wawe na ulinzi makini, wakaweka mipango ya kukatiana vipande vipande. Nehemia na wajenzi wakashika silaha za mikuki, ngao, pinde na dirii wakiendelea na kazi. Wakapata baragumu maana walikuwa mbalimbali ili kama ikibidi kupeana ujumbe watumie njia hiyo. Hawakuvua nguo zao walipolala, wakaenda na silaha zao hata walipokuwa wakiteka maji.



Nehemia akawausia watu wasitoze riba kwa ndugu zao wala kuuza ndugu zao. Hata leo ni dhambi kuwakopesha watu kwa riba kubwa. Shauriana na wale wanaompenda Mungu kile ambacho ni cha haki pale unapoishi. Yawezekana ukawa unawadhulumu wale wasiojiweza kabisa, na nyuso zao zinamtazama Baba yao mbinguni daima, nao wakisali, Mungu atawajibu. "Mungu wetu atatupigania," ulikuwa usadikisho wa Nehemia katikati ya mashambulizi ya maadui. Na imani hii ndiyo itayowatunza watu wa Mungu katika nyakati za taabu. Mungu Yu pamoja nasi, ila je, Sisi tu karibu na wenzetu pia au tunawaonea?

Kadiri watu wa Mungu wanavyojitahidi zaidi kufanya mapenzi ya Mungu, ndivyo adui anavyozidisha jitihada zake za kukatiza kazi yao. Shetani hawashambulii wale wasiofanya jambo lolote linalosumbua ufalme wa giza, lakini huwashambulia wale wanaofanya mapenzi ya Mungu. Mtu anaweza kufikiri kwamba kwa sababu Nehemia alisali na kumtegemea Mungu, yeye na watu hawangelazimika kufanya lolote kuhusu hali yao ngumu. Ni muhimu kujifunza kwamba Mungu anatazamia watu Wake wafanye kila wawezalo kwa upande wao na kumtegemea kikamilifu ili awalinde. Ni kwa kufanya hivyo ndiyo Mungu huwapigania. Maneno ya kutia moyo kutoka kwa viongozi yana nguvu wakati wa shida. Nehemia aliwatia moyo watu kwa maneno haya, "Msiwaogope hao, mkumbukeni Bwana"

Sanbalati alituma ujumbe wakutane uwandani ili wamdhuru Nehemia lakini yeye alijibu, "Hii ni kazi kubwa ninayoifanya mimi, hata nisiweze kushuka; mbona kazi ikome, hapo ninapoicha niwashukie?" Mwishowe hawa maadui walichoka. Nehemia akamaliza kazi. Watu wakakusanyika na Ezra mwandishi akaleta torati ya Musa mbele ya kusanyiko. Akasoma mapambazuko hadi adhuhuri mbele za watu. Ezra akamhimidi BWANA, Mungu mkuu, na watu wakaitika, Amina, Amina. Wakainua mikono kisha wakasujudu. Watu wengine wakaomboleza kwa huzuni kwa sababu walikuwa wamesahau torati ya Mungu na kufanya uovu. Watu walichomwa mioyo yao. Ezra akawaambia waende kwao na kusherehekea, wala wasihuzunike, maana wamegundua makosa yao na kuungama mbele za Mungu, Naye amewasaidia kumaliza kazi kubwa. Akawaambia, "Furaha ya BWANA ni nguvu yetu."

Akawaambia hii siku ni takatifu, wala msihuzunike. Siku ya pili walikusanyika tena na kusoma torati, wakagundua sikukuu ya vibanda wakaenda kukata matawi na kukaa vibandani siku saba. Tokea siku za Yoshua walikuwa hawajafanya sikukuu ya vibanda au makambi. Wengi hata siku hizi husherekea siku hii, Je, kanisa lako lina sikukuu ya vibanda?

Ezra akamsifu BWANA na kumrudishia utukufu, na akurudia maneno haya "WEWE Ndiwe BWANA Mungu, uliyemchagua Abramu na kumtoa Uri wa Wakaldayo…" akaendelea mpaka kutaja dhambi zilizofanya wachukuliwe mateka. Wakafanya agano na Mungu kuacha uovu, ili wawe huru na wabarikiwe. Watu wa koo tofauti wakatia muhuri wa agano hilo. Nehemia alikaa miaka 12 Yerusalemu, kisha akarudi tena kumtumikia mfalme, na kuja kutazama tena baadaye. Alisaidia hata mambo ya jamii, kama kusaidia familia bila kutoza riba. Akawaondoa watu wasiostahili waliokuwa wamepewa vyumba hekaluni. Watu walianza kumrudishia Mungu zaka na matoleo ya sadaka.

Maandiko yanatuhimiza "Kuomba bila kukoma." Hii haimaanishi kwamba tunapaswa kutumia muda wetu wote tukiwa tumepiga magoti yetu katika maombi rasmi, La! Bali Inamaanisha kwamba lazima tuishi na kumtumikia Bwana wetu katika mazingira ya maombi yaliyo rasmi na yasiyo rasmi (structured and unstructured), rasmi na yasiyo rasmi, yenye mpangilio na yasiyo na mpangilio, mfano ukiwa kwenye basi au safarini, ukiwa kanisani, ukiwa darasani, ukiosha vyombo, na si lazima kufumba macho wakati huo , ila unaweza kuinua mikono mitakatifu kama Biblia inavyoshauri ikibidi, usifikiri ni mambo ya dini fulani kuinua mikono, (1Tim2:5) hapana! Hutakuwa umekiuka sheria za Biblia kuinua mikono bila hasira wala magomvi, hata hivyo polisi akisema "mikono juu -hands up" si utaiweka? Basi kwanini usimwinulie mikono Mungu na kujisalimisha Kwake! Siku moja Kila goti litapigwa na kila ndimi itakiri Masihi ni Bwana).

Maombi ni njia ya mawasiliano kati ya nafsi zetu na MUNGU. MUNGU huzungumza nasi kupitia Neno Lake; tunamwitikia Neno Lake anapozungumza kupitia maombi yetu, Naye hutusikiliza daima. Hatuwezi kumchosha au kumlemea kwa mawasiliano yetu ya mara kwa mara ya mioyo yetu kwenda kwa moyo Wake. Tumefika kwenye nyakati ngumu. Matukio katika ulimwengu wetu yanamuhitaji kila mfuasi wa Kristo kuwa na bidii kabisa ndani ya uhusiano wake na MUNGU. Ili kuimarisha uhusiano huu na kutosheleza mahitaji yetu ya kihisia, kijamii, kimwili, kiuchumu na pia kiroho, ni lazima tujifunze nguvu ya maombi. Ni lazima tumsihi Bwana, kama wanafunzi wa awali, tukisema, "Bwana, tufundishe kuomba." Lazima tuseme kwa kusisitiza mambo matatu muhimu katika Maombi, nayo ni maombi yetu yawe ya Dhati, ya bidii na Usongo/ari (Earnest and Fervent Prayers). Hebu yafanyie utafiti maneno haya yana maana gani maana yamesheheni tunu kubwa, ambayo mpaka leo nasi tunajikanyaga kuyaelewa, tunaomba utuandikie na kutumegea nasi upatapo uelewa wake tafadhali sana! Mara nyingi watu hujiita Prayer Warrior wakimaanisha wapigana vita vya maombi au ni mashujaa wa maombi. Huduma ya Maombezi au Intercessory Prayer yaweza kufanywa na watoto na vijana pia! Maana Mungu ni Baba yetu na tunaweza kuzungumza Naye wakati wowote na kuleta shida za wenzetu na zetu. Tuandike mahali ili tukijibiwa

tusisahau kutoa shukurani, na shajara linasaidia kutukumbusha wema wa Mungu!

*Wakati Ubinafsi unapokufa, kutakuwa na uamsho wa hamu kubwa kuhusiana na wokovu wa wengine, - matamanio ambayo yatasababisha juhudi za kudumu na zenye uvumilivu katika kutenda mema. Kutakuwa na kupanda kando ya maji yote; na dua ya dhati, zizochoka, maombi ya kudumu, yataingia mbinguni kwa ajili ya nafsi zinazoangamia.

---

Nehemia alikuwa na huzuni kwa sababu gani? Mfalme aliyekuwa anatawala aliitwa nani? Mfalme alimpa nini Nehemia? Kwa nini Nehemia na wajenzi walishika silaha? Sanbalati alituma ujumbe gani?

**SIKU YA 150**
**(Mei 29)**

# Nabii Isaya - Mwaliko wa Njooni tusemezane



Nabii Isaya aliandika takribani mwaka wa 700KK. Isaya alikuwa anatoka ukoo wa kifalme. Isaya maana yake ni 'Wokovu ni wa BWANA.' Kitabu cha Isaya kinaitwa kitabu cha injili cha Agano la Kale, kwa sababu ya unabii wa Masihi. Manabii walioishi wakati mmoja na Isaya ni Hosea na Mika. Nabii hatabiri ya mbeleni tu, ila anazungumza na watu kwa niaba ya Mungu. Hapa taifa linaitwa lirudi kwa Mungu. Israeli ilikuwa imefanya uovu. Walichonga miti, ambayo vipande vingine walitumia kama kuni, vipande vingine wakajengea na vingine wakaviabudu. Masikitiko makubwa. Israeli lilikuwa taifa tajiri na lenye nguvu, lakini likageuka kuwa maskini, kwa miaka 200 tu. Hii ni kwa sababu ya kuasi maagizo ya Mungu na kuabudu miungu migeni. Walivunja amri za Mungu. BWANA alikuwa ametuma manabii wengi miaka nenda rudi, ili wajirudi kutoka katika njia za uovu na kutunza amri, na maagizo ya BWANA, lakini walishupaza shingo zao, wakaendelea kuchonga sanamu na kuziabudu. Kama wangeendelea kuwa waaminifu kwa Mungu, baraka hizi zingekuwapo kwao hata leo. Wangefurahia heshima na utajiri, na BWANA angewakinga na uovu toka kwa maadui zao. Miji yao ingekuwa mifano ya uzuri, mafanikio na mpangilio. Makosa yalikuwa mazito waliyofanya, na gharama yake ilikuwa nzito pia.

Nusu ya kwanza ya kitabu inatoa hitaji la wokovu; nusu ya pili inatoa unabii wa Mwokozi. Anaziita mbingu na nchi kushuhudia kile anachosema. Kwanza, ni lazima tufahamu hali yetu, kisha tutakuwa katika hali inayofaa kujinyenyekeza mbele za Mungu na kuomba msamaha, utakaso na nguvu za kupinga majaribu na kuishi maisha safi. Mungu hapendezwi na taratibu za dini zisiz na unyofu wa moyo ndani yake; Anataka ibada ya Kweli ya moyoni na mahusiano yaliyo hai, na yenye kuchangamka na kila mmoja wetu. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu Mpendwa kwa kutujali sana hata kuonyesha dhambi yangu na kisha anipe dawa. Daima napaswa kuwa tayari kufuata anaponiongoza. Katika Jina la Yesu, Amina.

Isaya alizungumza maneno ya kuonya na kuwatia moyo watu wake. Isaya aliishi wakati wa wafalme Uzia, Yothamu, Ahazi, na Hezekia, wafalme wa Yuda. Hii ina maana aliishi wakati wa wafalme saba wa mwisho wa Israeli, yaani kuanzia Yeroboamu wa pili mpaka Hoshea. Unabii wake si wa Yuda tu bali Moabu, Dameski, Misri, Tiro, Edomu, Uarabuni, Babeli, Ufilisti na hata anguko la Shetani mbinguni Isaya 14. Wafalme Hezekia na Senakeribu wanazungumzwa hapa, na jinsi Hezekia alivyoponywa ugonjwa wake, akasahau kutoa ushuhuda wa matendo makuu ya Mungu na akaonesha hazina au fahari yake tu.

Kupitia Isaya, BWANA alisema, "Nimewalisha watoto na kuwalea, nao wameniasi. Ng'ombe amjua bwana wake, na punda ajua kibanda cha bwana wake; bali Israeli hajui, watu wangu hawafikiri. Ole wake taifa lenye dhambi watu wanaochukua mzigo wa uovu, wazao wa watenda mabaya, watoto wanaoharibu, wamemwacha BWANA, wamemdharau Yeye aliye Mtakatifu wa Israeli, wamefarakana na kurudi nyuma. Mbona mnataka kupigwa hata sasa, hata mkazidi kuasi?… nchi yenu ni ukiwa; miji yenu imeteketezwa kwa moto; nchi yenu wageni wameila mbele ya macho yenu … binti sayuni ameachwa kama kibanda katika shamba la mizabibu, kama kipenu katika mashamba ya mitango kama mji uliotekwa." Kwa sababu ya kutotii, Bwana aliwauliza ni kwa nini wanaleta sadaka nyingi mbele zake? Ni za nini hizo? BWANA aliwataka wajioshe na kujitakasa dhambi zao, watake hukumu ya haki, kwa aliyeonewa, mjane, na yatima. Akawaambia, "Njoni tusemezane, asema BWANA. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji … Bali mkikataa mtaangamizwa kwa upanga."

Katika mwaka aliokufa mfalme Uzia, Isaya alimwona Bwana ameketi katika kiti chake cha enzi, kilichoinuliwa sana. Akaona maserafi, kila mmoja akiwa na mabawa sita, mawili walifunika uso, mawili wakafunika miguu na mawili yalitumiwa kuruka. Hawa walisifu utukufu wa Mungu wakisema, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni BWANA wa majeshi, dunia yote imejaa utukufu wake." Akaona hekalu limejaa moshi wa utukufu wa BWANA ndipo alipolia akisema, "Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, BWANA wa majeshi." Serafi mmoja aliruka na kaa la moto na kumgusa kinywa chake, akamwambia "uovu wako umeondolewa na dhambi yako imefunikwa." Naye akasikia BWANA akisema,"Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?" Isaya akajibu kwa unyenyekevu, "Mimi hapa, nitume mimi." Ndivyo Isaya alivyoanza kazi, njozi hii haikuondoka mawazoni mwake. Katika nyakati za taabu,

alijua kuwa BWANA Ndiye Mwenye enzi na anatawala. Akazungumza faraja kwa watu kwamba kuna siku Mungu atatuma mkombozi. "Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa Jina Lake, Mshauri wa ajabu, Mungu Mwenye nguvu. Baba wa milele, mfalme wa amani. Maongeo ya enzi Yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe."

Akawaambia watu Maneno ya faraja kama vile, "milima yaweza kuondoka ila fadhila zangu hazitaondoka kamwe." Akawapa watu maonyo akisema, "Mtafuteni BWANA maadamu anapatikana." Isaya anatuelezea kuhusu mbingu katika Isaya 35, 65 na 66. Vilema wataruka ruka, vipofu watafumbuliwa macho, viziwi watasikia. Mchungaji mmoja rafiki yetu alituelezea jinsi atakavyofurahia nyama ya nguruwe huko mbinguni, maana za hapa duniani zina ladha tamu. Je, za huko juu zitakuwaje? Nilikumbuka fungu la Isaya kwamba hakutakuwa na kifo mbinguni wala katika nchi mpya. Simba atakula majani kama ng'ombe na mbwa-mwitu na mwana-kondoo watalisha pamoja. Jingine ni kwamba nguruwe si nyama ya kula, kutokana na Maandiko!

Isaya anatukumbusha tupige kelele tusiache, tupaze sauti, kuwasaida watu wanapofanya makosa. Anatukumbusha, miguu mizuri ni ya yule anayepeleka habari njema za ufalme wa Mungu, habari za amani na wokovu. Je, wewe unataka kuwa na miguu mizuri? Basi miguu mizuri ni zaidi ya maumbile yanayofurahisha macho au rangi za kupaka. Ni ile inayoondoka na kuangaza maana nuru imetujia ya Neno la Mungu, tusikae kimya bila kuwaambia wengine maana giza kuu litafunika kabila za watu, bali BWANA atakuzukia wewe na utukufu Wake utaonekana juu yako, na mataifa au watu wengine watakuja wapate nuru yako ambayo ni Neno la Mungu. Japo u mtoto mdogo, BWANA amekupatia Roho Wake, amekuita ili uwaambie watu wengine habari njema, kuwapa kupona wale waliovunjika moyo, kuwafuta machozi wanaolia, kuwaweka huru waliofungwa, na kutangaza kwamba Yesu Kristo anarudi. MUNGU Yuko radhi na Yuko tayari kusikiliza na kujibu maombi yetu yanayotoka moyoni katika hali zote ni jambo lenye kutia moyo sana. Yeye ni Baba Mwenye upendo ambaye huzingatia wakati mambo yanaenda vizuri na wakati mabadiliko ya maisha yanapotuletea mapigo yenye kuhuzunisha, yaliyo magumu, na ya kutisha. Tunapojisikia kulia, "MUNGU, uko wapi?" Ni vizuri kujua kwamba Yeye Yupo karibu kupitia kuomba. Isaya alikuwa na wakati mgumu kwaajili ya uasi wa wafalme na raia zake. Alipewa Ujumbe mzito, nasi leo tumepewa ujumbe mzito kama Isaya. Yabidi tushikamane na mbingu katika kuutangaza Ujumbe huu wa Masihi.

*Oh, jamani kama sala ya dhati na ya imani ingetokezea kila mahali, Nipe roho zilizozikwa sasa kwenye uchafu wa makosa, la sivyo nife! Walete kwenye ujuzi wa Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu.

---

Isaya alikuwa na uhusiano gani na ufalme? Taja unabii ambao Isaya alisema kuhusu Masihi? Mwaka aliokufa Uzia Isaya aliona nini? Kuna malaika wa aina ngapi? Mungu akisema nimtume nani, utajibuje? Kwa nini utajiri wa Israeli ulipotea?

**SIKU YA 151**
**(Mei 30)**

# Ujumbe Zaidi wa Isaya



Israeli, ambalo lilikuwa ni taifa teule, lilikuwa na kiburi, na Isaya anawafananisha na binti au wanawake wenye kiburi, wenye kwenda kwa shingo zilizonyoshwa, na macho ya kutamani, wakienenda kwa hatua za madaha, na kuliza njuga kwa miguu yao. Onyo lilitolewa kuwa BWANA atawapiga kwa upele utosini na kufunua utupu wao." Bwana atawaondolea uzuri wa njuga zao, na pete za masikioni, vikuku, taji, dusumali, mafurungu, vibetwa, marashi, pete, mavazi ya sikukuu, vifuko, vioo vidogo, na kitani nzuri. Badala ya manukato kutakuwa uvundo, na badala ya mishipi, kamba; na badala ya nywele zilizosukwa vizuri, upaa; na badala ya nguo nzuri, magunia, na chanjo mbaya mwilini. Wanaume wataanguka kwa upanga na kutakuwa na kuomboleza.

Isaya alijulikana kama nabii mkubwa, kwa sababu kitabu chake ni kirefu, kupita vitabu vingine vya unabii. Isaya ni kitabu cha Injili cha Agano la Kale. Injili ni habari njema za ukombozi wa mwanadamu kupitia katika Yesu Kristo aliyetabiriwa katika kitabu cha nabii Isaya. Habari njema ni Yesu kuzaliwa, kuishi na watu, kufa na kufufuka. Wakati nabii Isaya akiendelea kuzungumzia utumwa waliokuwa nao, alisisitiza pia kuja kwa masihi na kutuondoa katika utumwa wa kiroho ambao ndio mzito na wenye athari kubwa zaidi hata kushinda ule wa kimwili. Maana tusipotoka kwenye utumwa huu, tutapotea milele. Nabii Isaya alioneshwa mateso ya Masihi na maisha atakayoishi katika Isaya 53, "Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama Mtu ambaye watu humficha nyuso zao. Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. Hakika ameyachukua masikitiko yetu, ametwaa huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa; Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu Yake maovu yetu sisi sote. Alionewa lakini alinyenyekea, wala hakufunua kinywa Chake; … Na maisha Yake ni nani atakayesimulia? … Alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu. Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya, … Naye atayachukua maovu yao… Akahesabiwa pamoja na hao wakosao." Unabii huu watu walipousoma baadaye, walijua kazi ya masihi, na atavyokuja na

kuokoa watu. Nasi leo tusome huu unabii, na tumkubali ili aone mazao ya taabu aliyoipata na kuridhika, na kutufanya wengi tuwe wenye haki, na siku moja tuingie mbinguni Tutapanda bustani na kufurahia kazi ya mikono yetu milele. Kama kuna vitu tunavyopenda kwa mioyo yetu kwenye familia yetu ni bustani! Tutakuwa wazao wa hao waliobarikiwa, na kabla hata hatujaomba tutajibiwa. Je, haitakuwa furaha kwetu kupapasa simba, na kuishi na wanyama hawa waliokuwa si wakali kabla ya dhambi? Hakutakuwa na kitu cha kutudhuru tena. Itakuwa mbingu na nchi mpya. Tutakutanika kwa ibada mwezi mpya hata mwezi mpya, na Sabato hata sabato kuabudu mbele Zake" asema BWANA.

Basi BWANA atalinda wale wote ambao mioyo yao imemtegemea, katika amani kamilifu, kwa kuwa wanamtumaini. Hebu tumtegemee BWANA na kumtumaini.

Isaya anazungumzia kurudi toka utumwani Babeli kisha anamalizia na unabii wa mbingu mpya na nchi mpya, huko hakuna vita tena; wala kuteseka, wala kuumizana, wala kupigana, wala hofu, wala mahangaiko, wala shida, njaa, kiu, wala huzuni, wala kilio, wala kifo. Watu watakuwa marafiki kila mahali. Huo ndio ulikuwa ujumbe mzuri wa Isaya wakati wa shida nyingi. Nasi leo tunaishi wakati huu wa shida, tujipe moyo na kuutafuta uso wa BWANA, na "kama vile mama anavyofariji watoto Wake, ndivyo BWANA atatufariji sisi," na mioyo yetu itafurahi na mifupa yetu itasitawi.
Weka mahitaji yako, furaha yako, huzuni zako, wasiwasi wako, na hofu zako mbele za MUNGU. Hauwezi kumlemea; hauwezi kumchosha. Yeye Anayehesabu nywele za kichwa chako hayuko tofauti juu ya mahitaji ya watoto Wake (hujali mahitaji ya watoto Wake). "Bwana ni mwingi wa huruma, ni mwingi wa rehema." Yakobo 5:11. Moyo Wake wa upendo unaguswa na huzuni zetu na hata sisi tunavyozitamka. Mpelekee kila kitu kinachotatanisha akili. Hakuna lililo kubwa Kwake kustahimili, kwani Yeye Ndiye anayeshikilia walimwengu, Anatawala mambo yote ya ulimwengu (mbingu na nchi Universe au malimwengu yote). Hakuna jambo lolote ambalo kwa njia yoyote ile linahusu amani yetu ni dogo sana Kwake hata asilitambue. Hakuna sura katika uzoefu wetu ambayo ni nyeusi sana Kwake hata asiweze kuisoma; hakuna wasiwasi ulio mgumu sana Kwake hata asiwe kuutatua. Hakuna janga liwezalo kumpata hata mdogo kabisa kati ya watoto Wake, hakuna mahangaiko yoyote yanayosumbua nafsi, hakuna furaha ya shangwe, hakuna sala ya unyoofu inayotoka midomoni, ambayo Baba yetu wa mbinguni haioni, au ambayo Yeye haizingatii mara moja. "Yeye huwaponya waliovunjika moyo, na kufunga majeraha yao." Zaburi 147:3. Mahusiano kati ya MUNGU na kila nafsi ni dhahiri na yamejaa (ni makamilifu) kana kwamba hakuna nafsi nyingine duniani inayoshiriki ulinzi Wake, au nafsi nyingine ambayo kwayo alimtoa Mwanawe Mpendwa kwa ajili Yake.

*Anzeni kuombea roho; njooni karibu na Kristo, karibu na ubavu Wake unaotoka damu. Hebu roho ya upole na utulivu iyapambe maisha yenu, Hebu maombi yenu ya dhati na bidii, yaliyopondeka, ya unyenyekevu yapande Kwake kwa ajili ya hekima ili mpate kufanikiwa katika kuokoa sio nafsi zenu tu, bali na nafsi za wengine.

---

Mbinguni kuna mambo gani mazuri? Isaya 53 inasemaje kuhusu Yesu au Masihi? Binti sayuni ana tabia gani? Kwa nini mbinguni kutakuwa hakuna kifo?

**SIKU YA 152**
**(Mei 31)**

# Ujumbe wa Yeremia Nabii - Baruku Mwandishi - 625 KK



Yeremia alionya juu ya uharibifu uliokuwa unakuja juu ya Yuda na kwamba taifa liungame na kuacha uovu, na kumrudia Mungu. Anatukumbusha kwamba, "moyo ni mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha, ni nani awezaye kuujua?" Alipewa ujumbe mzito kwa watu wa Yuda na Yerusalemu. Japo aliipenda Yuda, lakini alimpenda Mungu zaidi. Japokuwa ujumbe ulikuwa wa kusikitisha aliutoa, na kuomba rehema. Hata nasi tunapaswa kumtii Mungu, hata katika hali ngumu kwani katika mambo yote, Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani wale walioitwa kwa kusudi Lake. Mwandishi wa nabii Yeremia aliitwa Baruku. Huyu alikubali kuteseka japo alitoka katika familia yenye uwezo, ilimradi amsaidie nabii kufanya kazi yake. Wengine wahusika wakuu katika kitabu hiki ni wafalme wa Yuda, mfalme Nebukadreza, Warekabi na Ebedmeleki, Mkushi. Baba yake Yeremia alikuwa Kuhani Hilkia.

Mfalme mwema Yosia alipouawa na Farao-Neko wa Misri, kulikuwa na kuchanganyikiwa kwingi katika ufalme wa Yuda. Ashuru iliyokuwa inamiliki pengi, ilikuwa imevunjwa pia, hata mji wake mashuhuri wa Ninawi ulikuwa umeharibiwa. Misri na Babeli zilikuwa vitani, zikigombania vipande vya Ashuru. Farao-Neko alimchukua mfalme Yehoazi, mfalme huyu alitawala kwa miezi mitatu tu. Nabii Yeremia aliinuka kufanya kazi yake wakati wa Yosia, mfalme wa Yuda. Pia alifanya kazi wakati wa Yehoyakimu mwana wa Yosia na Sedekia. Neno lilimjia likisema, "kabla sijakuumba katika tumbo, nalikujua, na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa; nimekuweka kuwa nabii wa mataifa." Yeremia alikuwa kijana mdogo, akasema, "Aa BWANA, siwezi kusema; maana mimi ni mtoto." Lakini BWANA akamwambia, "Usiseme mimi ni mtoto, maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila Neno nitakalokuamuru, usiogope kwa sababu ya hao maana Mimi Nipo pamoja nawe nikuokoe asema BWANA." Ndipo BWANA akanyosha

mkono wake aguse kinywa chake na kumwambia kuwa ametia Maneno Yake kinywani mwake, akasema, “Nimekuweka leo juu ya mataifa na juu ya falme, ili kung’oa na kubomoa, na kuharibu, na kuangamiza; ili kujenga na kupanda.” Watoto wadogo wajue kuwa wao pia ni watumishi wa Mungu. Yeremia aliitwa akiwa mtoto, hata wewe Mungu akikuita, uwe tayari wakati wote, ruhusu mikono yake iguse midomo yako, usiogope.

Yeremia aliishi kabla na baada ya Yuda kuchukuliwa utumwani Babeli. Alilia machozi mengi, na anajulikana kama nabii anayelia. Aliandika kitabu cha maombolezo. Alilia Yerusalemu kuwa watu wote hodari wamechukuliwa, na mji umebaki ukiwa. Baadaye Yeremia aliwaandikia barua mateka waliokuwa Babeli kwamba wajenge nyumba na kuishi, wapande bustani na kula matunda, na kuoza wana wao. Wauombee amani mji ule wanaokaa, na wana wao watakaa kule miaka sabini, kisha watarudi kwao.

Yeremia amezungumzia pia, watumishi wa Mungu, ambao wanapokea mshahara lakini hawako tayari kuchunga kondoo wake au watu wa Mungu.

BWANA akamwambia Yeremia aende kwa mfinyazi, ili ajifunze kwamba BWANA ni mfinyanzi, nasi ni udongo. Je, udongo waweza kumwambia mfinyazi afinyange chombo kwa namna gani? Akamwambia avunje gudulia, na kusema ndivyo atakavyovunja watu hawa wanaojifanya sanamu za Baali na kupitisha watoto wao kwenye moto. Kama vile mfinyazi avunjavyo chombo kisichoweza kutengenezwa tena, ndivyo BWANA atakavyofanya wale wasiomtii. Pashuri kuhani aliposikia utabiri huu, akampiga Yeremia na kumweka kizimbani penye lango. Yeremia akamwambia Pashuri na watu wake wataenda utumwani. Yeremia akalia, “Ee BWANA umenihadaa … nimekuwa kitu cha kuchekesha, mchana kutwa kila mtu hunidhihaki”, maana kila alipozungumza alilia na kupiga kelele kuhusu dhuluma na uharibifu. Mara zingine alifikiri anyamazae maana watu wanamdhihaki, ila akasema akinyamaza, kuna moto unawaka kwenye mifupa yake nao unamsukuma awape watu habari za maonyo ya uharibifu unaokuja na wito wa kutubu, yaani, hakuweza kujizuia kutoa ujumbe aliotumwa na BWANA.

Yeremia akamwambia mfalme Sedekia, Mungu anataka amtii mfalme Nebukadreza na atunze ahadi yake; lakini alikataa kumtii. Wakaldayo waliporudi tena, kwa vile hakutoa kodi au kutaka kuwa chini yao, Sedekia akakimbia nje ya mji. Nebuzaradani alimkimbiza, akamshika na kumchukua mpaka Babeli, kwa Nebukadreza. Kule watoto wake waliuawa mbele ya macho yake na yeye mwenyewe akapofushwa macho yake. Ingekuwa heri kama angesikia maneno ya Yeremia. Babeli ilihusuru mji, na kukawa na njaa kubwa. Ilikuwa imepita miaka 400 toka Daudi atawale, na mambo yalikuwa tofauti kabisa.

BWANA akamwambia Yeremia aweke kongwa shingoni mwake ili kuonesha kwamba mataifa wamewekwa kuwa kongwa lao. Hanania akatoa kongwa hili, na BWANA akasema sasa Yuda watawekewa kongwa la chuma. Hanania, nabii wa uongo aliwatumainisha Yuda kwa maneno ya uongo na hilo lilifanya afe.

Yehudi, alilisoma gombo mbele ya mfalme Yehoyakimu, lakini badala ya kunyenyekea na kutubu, alilichoma moto, japo watu walimsihi asiharibu Neno la Mungu.

Nabii Yeremia alitupwa kwenye shimo lenye matope. Ebedmeleki, Mkushi, akamwendea mfalme na kumweleza juu ya Yeremia, na mfalme akaamuru Yeremia atolewe shimoni. Ebedmeleki alichukua watu thelathini pamoja naye wakaenda kumtoa Yeremia shimoni.

Gedalia, aliwekwa kuwa liwali juu ya nchi ya Wayahudi wakati wameenda utumwani. Nebuzaradani, amiri wa jeshi la Babeli alimwambia Yeremia kuwa ana uchaguzi wa kukaa Yerusalemu na kulishwa na Gedalia au kwenda Babeli. Yeremia aliwaambia watu wasiende Misri au kokote. Lakini watu hawakusikiliza, na baadaye wakamwua Gedalia.

Mungu anajua mawazo anayotuwazia sisi. Aliwawazia mawazo ya amani wala si mabaya, kuwapa tumaini siku zao za mwisho. Aliwaambia, "Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, Nami nitawasikiliza." Mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote."

Yeremia analeta kundi la Warekabi waliokuwa watu wa kuhama-hama waliojulikana kwa kushika sheria kwao kwa ukali na kujiepusha na kunywa pombe, wakijenga nyumba, wakipanda mbegu, na kupanda mizabibu (Yeremia 35:6–7). Warekabi walikuwa waaminifu kutii sheria hizi katika vizazi vyote, tangu wakati wa Yehu (2 Wafalme 10:15) hadi wakati wa Yeremia (Yeremia 35:8–10)—zaidi ya miaka 200.

Warekabi walikuwa wazao wa Rekabu, pengine wanaohusiana na Wamidiani na familia ya Musa kwa ndoa (Waamuzi 1:16). Kulingana na Yeremia 35:6 , sheria kali za Warekabi ziliwekwa na mzao wa Rekabu aliyeitwa Yonadabu. Huyu ndiye Yonadabu yule yule aliyemsaidia Yehu kuondoa ibada ya Baali katika Israeli baada ya wakati wa Ahabu (2 Wafalme 10:15–27). Yonadabu alitekeleza sheria hizo, lakini wengi wanaamini kwamba alijaribu kuhifadhi maisha ya kizamani ya mababu zake waliohamahama (mfano mzuri watakuwa watu wanaoitwa Amish au Menno Simmons).

Mungu alitumia uaminifu wa Warekabu kuwafundisha watu Wake Israeli somo muhimu. Bwana alimwambia Yeremia, "Nenda kwa jamaa ya Warekabi ukawaalike waingie katika chumba kimoja cha kando cha nyumba ya BWANA na kuwanywesha pombe" (Yeremia 35:2). Twapaswa kuwa kama Warekabi kukataa kabisa pombe na kueleza maagizo ya Mungu ambayo yako mengi, kuhusiana na Pombe. Nasi tubaki kuwa waaminifu kwa mapokeo ya familia yetu ya mbinguni!

Hapa pia kuna somo la Warekabi, walivyokataa, katakata kunywa pombe. Mungu alimwambia Yeremia kwenda na kuwaambia watu wa Yuda wajifunze somo la utii wenye uaminifu wa Warekabi wana wa Yonadabu (Yeremia 35:12–14). Mungu alitofautisha utii wa Warekabu na kutotii kwa watu Wake Mwenyewe. Twapaswa kuacha njia zetu mbaya kama Waisraeli, kwani wao hawakulitii Neno la Mungu. "Wazao wa Yonadabu mwana wa Rekabu walitekeleza amri ambayo baba yao

aliwaamuru, lakini watu hao wa Israeli hawakumtii Yeye" (mstari 16).

Kama matokeo ya uasi wa kihistoria wa Waisraeli, Mungu aliahidi kuleta maafa juu ya taifa (Yeremia 35:17). Lakini Mungu aliipongeza familia ya Warekabi na kuwapa ahadi: "Yonadabu mwana wa Rekabu hatakosa kuwa na mzao wa kunitumikia" (mstari 19).

Kuna mengi ya kujifunza kutoka kwa familia hii. Warekabi walisimama kidete dhidi ya kujiingiza katika utamaduni wa wakati huo. Walipongezwa na Mungu kwa uaminifu na utii wao kwa baba yao. Warekabi ni kielelezo cha uimara. Mungu anatamani watu Wake waishi kwa utii na uthabiti Kwake Yeye.

Bwana ametupenda kwa upendo wa milele ndiyo maana ametuvuta kwa fadhili Zake. Zamani, hata kabla hatujamjua, Mungu amekuwa akituvuta Kwake. Mawazo atuwaziayo BWANA ni ya amani, ili kutupatia tumaini katika siku zetu zote. Basi tumuite kwa kumwomba, Naye atatusikiliza. Tukimtafuta kwa mioyo yetu yote tutamwona Naye atatutendea makuu.

Kwa hivyo, tunapojifunza Yeremia, tunahitaji kujiuliza maswali fulani:
1. Tunajua nini kuhusu Yeremia?
2. Ujumbe wake ni upi? Je ujumbe huu ni muhimu kwa maisha yangu leo?
3. Je, ninaweza kumwona Yesu katika sura hii?
4. Je, ninaweza kuona Pambano Kuu kati ya Kristo na Shetani katika sura hii?
5. Je, majibu yangu kwa ujumbe yatakuwaje?


*Kuna wengi ambao matumaini yamewatoka. Warudishie mwanga wa jua hawa. Wengi wamepoteza ujasiri wao. Zungumza nao maneno ya furaha na ya kuwachangamsha. Omba kwa ajili yao.

---

BWANA alimwambia nini Yeremia pale aliposema yeye ni mtoto? Kwa nini Yeremia anajulikana kama nabii aliyekuwa analia? Pashuri alifanya lipi baya? Ebed-meleki alifanya lipi zuri? Kauli "Moyo ni mdanganyifu na una ugonjwa wa kufisha" ina maana gani? Wana wa Rekabu walifanya jambo gani la kustaajabisha?

**SIKU YA 153**
**(Juni 1)**

# Ujumbe Zaidi wa Yeremia



Yote aliyotabiri Yeremia kuhusu Yerusalemu yalitokea. Watu waliochukuliwa kwenda uhamishoni walikuwa wengi, miongoni mwao ni Danieli, Anania, Mishaeli na Azaria. Jambo zuri ni kwamba hawa waliendelea kumwabudu Mungu katika nchi ya ugeni. Matatizo yao yaliwasogeza karibu zaidi na Mungu, hata walikuwa tayari kufa kwa ajili ya imani yao. Japokuwa wengi wamemwita Yeremia nabii mlizi, na hata naye akaandika kitabu cha Maombolezo, si yeye peke yake aliyekuwa akilia! Mungu wetu Naye amekuwa akililia watoto Wake waliojiweka kwenye machungu, na hata wakati mwingine ukisoma hiki kitabu cha Yeremia unashindwa kushangaa kwamba katika mstari huu ni Yeremia anayelia au ni MUNGU wetu Ndiye Anayelia! Hakika lile fungu la Yohana 3:16,17 ni la Haki kabisa, yaani kwenye Agano la Kale na Agano Jipya “Yn 3:16-17 yaani “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika Yeye”, Hakika Mungu wetu analia machozi kwaajili yetu tunapojiweka miibani au taabuni wenyewe, Hebu leo tunapoisikia sauti Yake, tusiifanye mioyo yetu kuwa migumu. Maagizo Yake ni kwa faida yetu na binadamu wenzetu! Mungu katika Sefania tatu pia, anatufurahia na kuimba nyimbo kuhusu sisi, pale ambapo hatujiumizi na kuumiza wengine, pale ambapo tuna upendo wa kweli, Hebu leo, na tuombe tuwe na huu upendo wa kweli, wa kumpenda Jirani yetu kama nafsi zetu, na kumpenda Mungu kwa mioyo yetu yote, kwa akili zetu zote, kwa nguvu zetu zote, na kwa roho zetu zote, kwa Jina lile tukufu la Masihi, Amina! Na ndipo dunia itakuwa nusu mbingu!

Bwana alisema, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, au tajiri asijisifu kwa mali zake, bali kila ajisifuye, ajisifu kwamba anamjua BWANA, na kwamba anatenda wema, na hukumu, na haki. Akawaambia kuwa hata ndege

angani wanajua wakati wa kuhama, lakini watu Wake hawajui. Yeremia anasisitiza watu Wake wasimtegemee mwanadamu zaidi ya Mungu, “amealaaniwa yeye amtegemeaye mwanadamu, yeye amfanyaye kuwa kinga yake. Lakini amebarikiwa yeye amtegemeaye Mungu, atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya mto.

Kitabu cha Maombolezo ni nyimbo au mashairi ya huzuni au ya kuomboleza. Jina linaonesha Yeremia kama nabii anayeomboleza. Aliandika baada ya Wababeli au Wakaldayo kuharibu Yerusalemu. Anasema nyuso za wazee hazipewi heshima, na vijana huyachukua mawe ya kusagia wakiwa na kazi saa zote wakati wanatawaliwa na falme nyingine. Hata wanawake wenye huruma wamewala watoto wao.

Nabii aliandika maombolezo baada ya Yerusalemu kuanguka mwaka 586 KK. Alitabiri kuanguka kwake na akaona kwa macho yake. Kitabu kinaonesha mfadhaiko wa moyo na kutufundisha kuwa kutomtii Mungu kunaleta mateso na maumivu mengi. Yeremia anamwambia BWANA huzuni zake na kuomba awaonee huruma. “Jinsi mji huu ukaavyo ukiwa, huo uliokuwa umejaa watu! Jinsi ulivyokuwa kama mjane. Yeye aliyekuwa mkuu kati ya mataifa.” Yeremia alijua wamefanya makosa, lakini huenda hakutegemea kuwa Mungu atatumia watu wanaoabudu miungu migeni kutoa adhabu kwa wale wanaomjua Mungu. Anasema, “Ni Huruma za BWANA kwamba hatuangamii, kwa kuwa rehema Zake hazikomi, ni mpya kila siku asubuhi, uaminifu Wako ni mkuu. BWANA Ndiye fungu langu, husema nafsi yangu; Kwa hiyo nitamtumaini Yeye. BWANA ni mwema kwao wamngojeao, kwa hiyo nafsi imtafutayo. Ni vyema mtu atarajie wokovu wa BWANA, na kumngojea kwa utulivu.”
Mungu anaona upumbavu huu kwa wengi wetu na kusema: “Kwa maana watu wangu ni wapumbavu, hawakunijua Mimi. Ni watoto wajinga, na hawana ufahamu. Wana hekima katika kutenda mabaya, lakini katika kutenda mema hawana maarifa.” (Yer. 4:22 NKJV).

Maombi:
“Mpenzi Mungu wangu, mimi ni mwalimu nitake au nisitake. Watu hujifunza kutokana na maneno na matendo yangu. Tafadhali nifundishe jinsi ya kuwa mwalimu bora anayekutuza Wewe. Waruhusu wengine kuona maneno Yako na matendo Yako kupitia maisha yangu na kwa kuvutiwa kwao, waje Kwako. Amina.”

*Kazi hii inakuhitaji uzilinde roho kama yule ambaye lazima utazitolea hesabu. Upole wa Kristo lazima uujaze moyo wa Mfanyakazi wa Sala ya Maombezi. Ikiwa una upendo kwa roho utaonyesha kujali kwa dhati kwa ajili yao. Utatoa maombi ya unyenyekevu, ya dhati, ya kutoka moyoni kwa wale unaowatembelea. Harufu ya upendo wa Kristo itadhihirishwa katika kazi yako. Yeye ambaye alitoa maisha Yake kwa ajili ya maisha ya ulimwengu atashirikiana na mtenda kazi asiye na uchoyo au ubinafsi kuweka msukumo juu ya mioyo ya wanadamu.

---

Uzuri wa kuwa mateka Babeli ulikuwa nini? Kitabu cha Maombolezo kinahusu nini? Yeremia anasema sababu pekee ya kujisifu ni nini? Kwa nini amelaaniwa yeye amtegemeaye binadamu?

**SIKU YA 154**
**(Juni 2)**

# Nabii Ezekieli



Ezekieli alichukuliwa mateka wakati Wakaldayo walipovamia Yerusalemu mara ya pili. Ezekieli aliishi wakati mmoja na Danieli. Ezekieli alipata njozi akiwa uhamishoni Babeli karibu na mto Kebari. Anazungumzia majukumu ya mtu binafsi, wakati Israeli walitegemea waokolewe pamoja, au kupotea pamoja. Mara nyingi Mungu alimwambia afanye vitendo ili kuwa ishara ya unabii wake. Ezekeli anaitwa na Mungu, "Mwanadamu," akiwakilisha wanadamu. Yesu aliitwa pia Mwana wa Adamu. Ezekieli aliwatia moyo kwamba utumwa wao utakwisha, na Mungu atawarudisha nyumbani. Nebukadneza aliwatendea wema, akawapa bustani za udongo wenye rutuba, kisha wakajijengea nyumba. Wengine waliishi mijini, na hata kupata utajiri. Wengine walifanya kazi kwenye nyumba ya mfalme au serikali yake, na kuwa watu wa kuheshimiwa sana, kama mawaziri.

Ezekieli mwana wa Buzi alikuwa na miaka 30 alipoanza kutabiri, na alianza huduma yake miaka mitano baada ya kuchukuliwa Babeli ambao ni kama mwaka 570 KK. Jina Ezekieli lina maana ya 'Mungu anatoa nguvu.' Ezekieli alihudumu kwa watu ambao walikuwa na "nyuso zisizo na haya na wenye mioyo migumu." Mungu aliahidi kuwarudishia utukufu wao baada ya adhabu au hukumu ili wote wajue kwamba "Yeye Ndiye BWANA".

Siku moja Ezekieli alipata njozi akaona mbingu zimefunuka na viumbe wanne, wenye sura nne na juu yao kulikuwa na kiti cha enzi cha Mungu cha vito vya yakuti samawi. Akaanguka kifudifudi, akasikia sauti ikisema naye. Viumbe hai wanne hivi

kwa kuonekana walikuwa na sura ya mwanadamu, na kila mmoja kilikuwa na sura nne, na mabawa manne. Miguu iliyonyoka na ilikuwa na rangi ya shaba ya kumetameta. Walikuwa na uso wa mwanadamu upande wa mbele, upande wa kulia uso wa simba, upande wa kushoto uso wa ng'ombe, na upande wa nyuma uso wa tai.

Mambo haya yalipita uwezo wake wa kuelewa kwani yalikuwa magumu sana hivi kwamba alichanganyikiwa. Lakini basi nabii huyo aliona upatanifu wa ajabu, kwa maana waliposonga wanyama hawa, kulikuwa na usahihi mzuri na upatano mkamilifu. "Roho" Anatajwa mara kumi katika sura tatu za kwanza za Ezekieli. Ni Roho Ndiye aliyetawala na kuratibu nguvu mbalimbali. Ni Roho Ndiye aliyeleta maelewano kutoka katika kile kilichoshangaza. Hakika Roho, Ndiye shujaa mkuu wa kitabu cha Ezekieli. Hata leo hivi, Roho wa Mungu Ndiye shujaa mkuu na Kiongozi katika kazi yetu. Tukumbuke kuwa Huyo anaweza kuleta utaratibu kutoka katika machafuko, maelewano kwenye mtafaruku, na umoja kwenye malumbano. Na uhai kutoka kwenye mifupa mikavu.

"Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho Wangu, asema Bwana wa majeshi" (Zek. 4:6).

Baadhi ya matendo aliyofanya ili kueleza ujumbe ni haya: Aliambiwa alale chini kwa ubavu wa kushoto kwa siku 390 na kisha kwa ubavu wa kuume siku arobaini. Kisha akaambiwa atwae ngano, shayiri, kunde, dengu na mtama na aweke kwenye chungu na kutengeneza mkate. Mkate huo ndio atakaokula kwa siku mia tatu tisini. Akaambiwa Asile zaidi ya robo kilo ya mkate kwa siku, na asinywe zaidi ya glasi tatu za maji kwa siku, ikionesha njaa au upungufu wa chakula. Akaambiwa auoke mkate huo juu ya mashonde ya mwanadamu. Hivyo ndivyo wana wa Israeli watakavyokula chakula kilichotiwa unajisi. Ezekieli akamsihi Mungu kwamba yeye toka ujana hajala kitu najisi, basi BWANA akamwambia atumie mashonde ya ng'ombe yaliyokauka. Akasema watakula mkate kwa kuutunza sana na kuupima, watastaajabu kwa kukonda kwa ajili ya uovu wao.

Ezekieli akaambiwa ajipatie wembe mkali akate nywele na ndevu zake. Kisha azipime kwa mizani. Theluthi ya nywele aziteketeze kati ya mji, na theluthi aipige kwa upanga na theluthi aitawanye ichukuliwe na upepo. Tafsiri ikawa theluthi watakufa kwa njaa, theluthi watakufa wakilinda mji, na theluthi watatawanyika na kufukuzwa na adui.

Akaambiwa afunge mizigo mchana watu wakimwangalia na atoboe ukuta wakiona na aweke mizigo begani na atoke nayo kwenye ukuta aliotoboa usiku. Atoke nayo mizigo hiyo ikimaanisha watachukuliwa mateka na watatoka kwa uchungu wakifunika nyuso zao, maana hawataona mji wao tena. Kisha Neno likamjia ale chakula, na kunywa maji akitetemeka na akivitunza visiishe. "Waambie watu wa Yerusalemu watakula na kunywa wakitetemeka kwa ushangao, nchi itakuwa ukiwa na njaa." Japo Ezekieli aliwaambia watu walimkejeli wakisema, "mbona siku zinakawia na maono hayatimizwi!" Kweli sikio la kufa halisikii dawa.

Ezekieli akaambiwa na Mungu kuwa atawasha moto msitu wa Negebu, na kula kila mti mbichi na mkavu, na hautazimika. Maadui watakuja na wataua wengi. Japo watu walimbeza wakisema "mtu huyu anasema mithali tu na hakuna linalotokea."

Kisha akaambiwa, akaoneshe kwa mkono wake kama analeta upanga kupiga mara mbili au tatu kwa kuwa wengi watapigwa na kufa. Upanga umenolewa na kusuguliwa, "piga kelele utoe sauti ya uchungu, Ee mwanadamu." Ndivyo watakavyofanyiwa na maadui zao.

Kisha akaambiwa kuwa mke wake ampendaye atakufa, lakini asiomboleze wala kulia, machozi yasichuruzike. Asononeke, ila si kwa sauti ya kusikika, asifanye matanga kwa ajili yake aliyekufa. Mke alikufa na Ezekieli akafanya kama alivyoagizwa. Alipoulizwa maana yake, akawaambia kuwa hekalu, na pia wana na binti zao walioachwa nyuma wataanguka kwa upanga, na wao wafanye kama alivyofanya, wasile chakula cha watu, wasilie, bali wawe na vilemba kichwani na viatu miguuni bila kuomboleza. Ila walie mioyoni mwao tu.

Mungu anatoa mfano wa Israeli na Yuda kama dada wawili waitwao Oholiba na Ohola waliokuwa wakienda na wanaume mbalimbali, bila kukaa kwa mume mmoja. Mungu anawachukulia watu Wake kama mwanamke safi, na wale wanaoenda kwa miungu mingine ni kama mwanamke anayemwacha mume wake na kwenda kufanya uzinzi au kuishi na wanaume wengine ambao hawakufunga ndoa nao. Mungu anataka tusiwe na miungu mingine, hii ni dhambi. Kuwa na miungu ni kutokuwa mwaminifu Kwake ambayo italeta athari kwenye maisha yetu, na ya binadamu wengine. Yeye anajua athari Zake kuliko sisi, hebu na tusikie, maana watu kama Sulemani walipuuza mwishowe walifikia hatua ya kutoa watoto wao kafara kwenye moto.

Akaambiwa atwae vijiti viwili, kimoja aandike Yuda na cha pili Yusufu, akaviunge pamoja na watakapouliza maana yake, awaambie kwamba atarudisha Yuda na makabila mengine pamoja, hawatakuwa vitu viwili tena, atawaokoa na kuwatakasa, watarudi wawe kama zamani na kuishi kwa amani wakijua kuwa "Yeye, "Ndiye BWANA."

*Omba Upate Baraka Ili Kuwabariki Wengine—Maombi yetu hayapaswi kuwa maombi ya uchoyo au ubinafsi, kwa faida yetu wenyewe tu. Tunapaswa kuomba ili tuweze kutoa. Kanuni ya maisha ya Kristo lazima iwe kanuni ya maisha yetu. "Kwa ajili yao," Yeye alisema, akizungumza juu ya wanafunzi Wake, "Najiweka wakfu, ili nao watakaswe." Yohana 17:19. Kujitoa huko huko, kujitolea nafsi kwa namna ile ile, utiifu uleule wa madai ya Neno la MUNGU, ambao ulidhihirika katika Kristo, lazima uonekane kwa watumishi Wake. Utume au misheni yetu kwa ulimwengu sio kujitumikia wenyewe, au kujifurahisha wenyewe; tunapaswa kumtukuza MUNGU kwa kushirikiana Naye katikakuwaokoa wenye dhambi. Tunapaswa kuomba baraka kutoka kwa MUNGU ili tuweze kuwasilisha kwa wengine. Uwezo wa kupokea huhifadhiwa kwa kutoa tu (tunapokea tu tukitoa). Hatuwezi kuendelea kupokea hazina ya mbinguni bila kuwasiliana na wale wanaotuzunguka.

⋆Omba Upate Baraka Ili Kuwabariki Wengine—Maombi yetu hayapaswi kuwa maombi ya uchoyo au ubinafsi, kwa faida yetu wenyewe tu. Tunapaswa kuomba ili tuweze kutoa. Kanuni ya maisha ya Kristo lazima iwe kanuni ya maisha yetu. "Kwa ajili yao," Yeye alisema, akizungumza juu ya wanafunzi Wake, "Najiweka wakfu, ili nao watakaswe." Yohana 17:19. Kujitoa huko huko, kujitolea nafsi kwa namna ile ile, utiifu uleule wa madai ya Neno la MUNGU, ambao ulidhihirika katika Kristo, lazima uonekane kwa watumishi Wake. Utume au misheni yetu kwa ulimwengu sio kujitumikia wenyewe, au kujifurahisha wenyewe; tunapaswa kumtukuza MUNGU kwa kushirikiana Naye katika kuwaokoa wenye dhambi. Tunapaswa kuomba baraka kutoka kwa MUNGU ili tuweze kuwasilisha kwa wengine. Uwezo wa kupokea huhifadhiwa kwa kutoa tu (tunapokea tu tukitoa). Hatuwezi kuendelea kupokea hazina ya mbinguni bila kuwasiliana na wale wanaotuzunguka.

---

Taja maigizo manne ambayo Ezekieli aliambiwa afanye ili watu wake wapate ujumbe? Sura nne za wale viumbe zilikuwa za namna gani?

**SIKU YA 155**
**(Juni 3)**

# Ujumbe wa Ezekieli Unaendelea

Ezekieli haitwi kuwahubiria watu wa mbali, bali watu wake. Kuwahubiria marafiki na familia yako kunaweza kuwa na changamoto. Hakika mwito wake ni mgumu kwani wale watu hawakusikia. Uinjilisti wenye ufanisi ni kazi ya Mungu; Yeye hazuiliwi na udhaifu wetu. Hii ni habari njema na ni habari ya kutatiza moyo pia. Inanyenyekeza kwa sababu hata kama wewe ni mzungumzaji mzuri zaidi na hodari wa kila ustadi katika uinjilisti, bila Roho wa Mungu hutafanikiwa kuwafikia waliopotea. Wito wetu kutoka kwa Mungu si tofauti sana leo na siku za Ezekieli. Mwitikio wetu unapaswa pia kuwa sawa—utiifu na kujisalimisha kwa Mungu kikamilifu kabisa. Kisha Yeye atakuja kwako na kufanya tofauti zote bora maishani mwako.

Walipokuwa Babeli, Wayahudi hawakuisahau nchi yao kamwe. Tafakari maneno ya Zaburi 137: "Kando ya mito ya Babeli ndiko tulikoketi,Tukalia tulipoikumbuka Sayuni Katika miti iliyo katikati yake tulivitundika vinubi vyetu Maana huko waliotuchukua mateka Walitaka tuwaimbie; Na waliotuonea walitaka furaha; Tuimbieni baadhi ya nyimbo za Sayuni.
Tuimbeje wimbo wa BWANA katika nchi ya ugeni? Ee, Yerusalemu nikikusahau wewe,
Mkono wangu wa kuume na usahau. Ulimi wangu na ugandamane
Na kaakaa la kinywa changu nisipokukumbuka. Nisipoikuza Yerusalemu zaidi ya furaha yangu iliyo kuu"
Ezekieli alitabiri Waedomi kushindwa. Tiro kuvamiwa na nchi zingine, na kutupwa isijengwe tena, na Misri haitatawala mataifa tena, na kisha wana wa Israeli watarudi kwao.

Katika huu uhamisho walianza kuitwa Wayahudi wakiwa mateka; ikiwa ina maana watu wa
Yuda. Wayahudi duniani kote walitokea hapa. Wayahudi na Waisraeli sasa watu wakisema neno hilo ni kitu kimoja sasa.

Ezekieli aliitwa awe mlinzi wa nyumba ya Israeli ili atoe maonyo kwa watu wa Mungu. BWANA anasema, "Nimwambiapo mtu mbaya hakika utakufa, nawe usimpe maonyo…mtu mbaya atakufa katika uovu wake, lakini damu yake nitaitaka kwako." Lakini akimwonya, naye hauachi ubaya wake, basi Ezekieli au sisi tutakuwa tumejiokoa roho zetu. Mara nyingi tunaona aibu kuwaambia au kuwaonya rafiki zetu wanapofanya jambo ovu, hata yale ya waziwazi. Pengine tunawaonea haya au tunaogopa kwamba nasi pia watatuambia tukifanya uovu. Ni vyema watuambie, ila tusinyamaze tukiona uovu, bali tusaidiane kwa upendo.

Kisha akaambiwa kuwa watamtia pingu, na ulimi wake utagandamana na kuwa

bubu, wala hatakuwa mwonyaji kwa vile ni wenye kuasi. Lakini baadaye BWANA akamwambia afumbue kinywa chake na yeye asikiaye na asikie maonyo ya BWANA, akataaye na akatae. Ameonya juu ya vitu kama mizani za uongo na zisizo za haki. BWANA alionya kuwa hata Nuhu, Danieli na Ayubu, ambao ni watakatifu, wakiwaombea watu haitasaidia, maana watajiokoa wenyewe tu. Hatuwezi kumpeleka mtu mwenye shingo ngumu mbinguni. Lazima mtu mwenyewe aamini na kutii. Tunaokolewa kwa neema ya Mungu, lakini sharti tuwe na imani, na pia imani yetu izae matunda, maana imani bila matendo imekufa.

BWANA aliwaita wazitakase Sabato Zake, kwani ni ishara kati ya Mungu na wanadamu, wapate kujua Ndiye BWANA Mungu wao. Sabato ni muhuri wa Mungu katika kazi Yake uumbaji, na ni amri aliyoitoa ili tukumbuke uumbaji.



Mungu alimchukua Ezekieli kwenye bonde lililokuwa na mifupa mikavu ya watu waliokufa, na Mungu akamwuliza, “Je! mifupa hii yaweza kuishi? Ezekieli akajibu “Ee Bwana MUNGU, wajua Wewe.” Bwana akamwambia kuwa mifupa ile mikavu iliwakilisha nyumba ya Israeli, na kuwa atoe unabii kwamba BWANA atatia pumzi ndani ya wana Israeli japo wamekufa, nao wataishi. Ezekieli akatoa unabii huu kama alivyoamriwa, na kukawa na mshindo mkuu, na tetemeko la nchi. Ile mifupa ikasogeleana, mfupa kwa mfupa mwenzie, na tazama nyama, mishipa, na ngozi ikatokea na kuifunika mifupa lakini haikuwa na uhai. Ndipo BWANA akatuma upepo uje toka pande nne na pumzi iwapulizie wale waliokufa. Pumzi ikawaaingia, wakaishi, wakasimama kwa miguu yao jeshi kubwa mno. Mungu akasema unabii huu ni wa kuwapa matumaini watu wake ambao walisema, “mifupa yetu imekauka, matumaini yetu yametupotea; tumekatiliwa mbali kabisa.” Mungu akasema atafunua makaburi yao na kuwapandisha, na kuwarejesha Israeli. Basi, tujue kuwa Mungu wetu anajua yote, na maarifa yote, na ana uwezo wa kufanya lolote tumwombalo, tunalohitaji maana Ndiye BWANA. Atatusaidia mioyo yetu ya jiwe iwe nyama, ili tunyenyekee na kumcha Yeye.

*Tunapoomba, “Utupe leo mkate wetu wa kila siku,” tunaomba kwa ajili ya wengine na pia sisi wenyewe. Na tunakubali kwamba kile ambacho MUNGU anatupa si kwa ajili yetu wenyewe tu. MUNGU hutukabidhi kama amana, ili tuwalishe wenye njaa.

---

Elezea kisa cha mifupa mikavu? Kwa nini Nuhu, Danieli na Ayubu hawawezi kuokoa mtu yeyote? Tusipomwambia mtu mwovu kosa lake, nini kitatokea?

**SIKU YA 156**
**(Juni 4)**

# Esta Awa Malkia

Kitabu cha Esta ni moja ya vitabu vinavyoelezea sehemu ya historia ya Wayahudi walipokuwa uhamishoni. Esta akiwa ni mmoja wa wahusika wakuu. Aliwasaidia Ezra na Nehemia kwa nafasi aliyokuwa nayo kama mke wa mfalme na dada yao wa nyumbani (home girl!).

Kitabu hiki kinahusu zamani za mfalme Ahasuero, aliyetawala sehemu ya dunia inayojulikana kama sehemu ya Ulaya, Afrika na Asia. Nchi yake asilia iliitwa Uajemi. Huyu alitawala baada ya wafalme Koreshi na Dario. Shushani ngomeni ilikuwa mji wake mkuu. Mfalme Ahasuero aliwafanyia maakida wake, yaani, viongozi, karamu kubwa, akaalika watu wa majimbo mbalimbali. Akawaonesha utajiri wake, utukufu na enzi yake kwa siku mia na themanini. Watu walikunywa bila masharti, kama mfalme alivyoamuru. Mfalme akaruhusu kila mtu afanye apendavyo. Mke wake, malkia Vashti, aliwafanyia wanawake karamu pia ndani ya nyumba ya kifalme Siku ya saba mfalme akiwa amefurahishwa na divai kwa kulewa alituma wasimamizi wake kumleta malkia wake Vashti, amwoneshe mbele ya mfalme akiwa amevaa taji, maana

alikuwa mzuri wa uso. Bali Vashti alikataa kuja na wale watumishi. Hatujui sababu za kukataa kwake, pengine alipaswa kuja amevaa nguo nusu, au alikosa adabu au aliogopa kuaibishwa kwa ulevi. Mfalme akaghadhabika mno, na kuwaambia wale wanaojua sheria na hukumu afanye nini? Nao wakamwabia, huyo Vashti "hakumkosa mfalme tu," bali viongozi wote na watu wote pia. Wakasema tendo hili litajulikana na wanawake wengine na hata wanaume wao watadharauliwa machoni pao, watakaposikia kuwa Vashti hakuja mbele ya mfalme pale alipoamuru hivyo.

Basi walitoa hukumu kuwa Vashti asije mbele ya mfalme tena, na umalkia wake, mfalme ampe mwanamke mwingine aliye mwema kuliko yeye. Basi mbiu ikapigwa na waraka ukaandikwa kwamba kila manamume atawale nyumbani mwake na siyo mke kumtawala mume. Hata leo ni kosa kwa mwanamke kumtawala mwanamume, kwani mume ni kichwa cha mke. Na hapa tunahitaji hekima, wanaume na wanawake, kwani kuwa kichwa ni jukumu zito, ila tukimweka Mungu kuwa kichwa, tutashinda.

Hasira za mfalme ziliisha na alipotulia alimkumbuka mke wake na aliyotenda na watumishi wakaona mfalme ana ukiwa, wakasema atafutiwe mke mwingine. Basi wakapeleka maagizo ya kutafuta wasichana wazuri vijana, mabikira, katika majimbo yote. Yule msichana ambaye angempendeza mfalme ndiye angekuwa malkia. Hegai akawatunza, akisimamia nyumba na vifaa vya utakaso.

Huko mji wa Shushani ngomeni kulikuwa na Myahudi wa Benyamini aliyekuwa wa uzao wa waliochukuliwa mateka pamoja na Yekonia mfalme wa Yuda, jina lake akiitwa Mordekai. Huyu alikuwa na binamu yake aliyemtunza kama mwanawe

aitwaye Hadasa (Esta) kwani alikuwa yatima. Esta alikuwa na umbo zuri na uso mwema na amri ya mfalme ilipotoka kutafuta malkia, wasichana wengi walikusanyika Shushani ili wapate bahati ya kuchaguliwa kuwa malkia. Mordekai alimpeleka Esta kwa Hegai aliyewalinda wanawake, Hegai alipendezwa na haiba ya Esta, akashughulikiwa kuliko kawaida ili kujitayarisha kwenye mashindano ya uzuri na kuwa malkia. Akapewa vifaa vya urembo, posho, na vijakazi saba waliokuwa haki ya kila msichana. Wale wasichana wakawekwa mahali pazuri, katika nyumba ya wanawake. Esta aliambiwa na binamu yake Mordekai kuwa asijitambulishe kuwa yeye ni Myahudi, pengine kuepuka ubaguzi. Mordekai alimtembelea Esta kila siku ili ajue hali yake na yale yatakayompata.



Wasichana walioenda walipopita mbele ya mfalme siku yao ikifika, hawakurudi makwao, bali walikuwa kama masuria wa mfalme. Hawa walikuwa wameharibiwa maisha. Mwandishi anasema mwanamwali akienda kwa mfalme, "Huenda jioni, na asubuhi hurudi nyumba ya pili ya wanawake," kama suria. Wala haingii tena kwa mfalme, isipokuwa amempendeza mfalme, naye akaitwa kwa jina. Hili ni jambo baya kwa msichana yeyote kumtokea, ila kwa sababu wafalme hawa wa dunia hawakumjali Mungu, walifanya yale waliyoona ni mema machoni pao wenyewe. Wasichana walikaa kule mwaka mzima, miezi sita kwa mafuta na manemane na miezi sita kwa manukato na vifaa vya utakaso kwa wanawake. Walifanyiwa urembo, na pia kufundishwa jinsi ya kujiweka kuwa mke wa mfalme, kwa mazungumzo, kukaribisha wageni, kuongoza vijakazi na hata mwonekano na majukumu kama mke wa mfalme. Ilipofika siku ya Esta kumwona mfalme, hakutoa masharti mengi ya kutaka vitu, ila vile Hegai alivyompangia. Esta alipata kibali kwa waliomwona, na alipopelekwa nyumba ya mfalme, mfalme akampenda kuliko wanawake wote, na akapata neema kuliko wote. Mfalme akamtia taji kichwani pake na kumfanya awe malkia badala ya Vashti. Mfalme akafanya karamu kubwa na kutoa msamaha kwa wafungwa na zawadi sawasawa na ukarimu wa mfalme. Mordekai alifanya kazi nzuri kama mzazi/mlezi, kwani alishika maagizo yake na yakafanya watu wakamwona ni msichana tofauti.

Mordekai alikaa mlangoni pa mfalme kama mlinzi, na siku moja alisikia wasimamizi wa mfalme Bigthana na Tereshi wakipanga kumwua mfalme. Mordekai alipojua alimwambia Esta, naye akamwambia mfalme. Jambo hilo lilipochunguzwa na ikaonekana kuwa ni kweli, wote wawili walitundikwa juu ya mti, na mfalme akaandika rekodi ya taarifa za mfalme.

Kisha mfalme akamwongeza cheo Hamani, Mwagagi wa Amaleki, ambaye mfalme wao mwovu aliuawa na nabii Samweli. Hamani alipokuwa akipita langoni, watu waliinama na kumsujudia, ila Mordekai hakufanya vile, watumishi wa mfalme walipomwuliza alisema yeye ni Myahudi. Hamani alipoona hasujudiwi alighadhabika sana, ila hakutaka kumfanyia ovu lolote Mordekai peke yake bali Wayahudi wote katika ufalme wa Uajemi. Hamani akaenda kumwambia mfalme kuhusu Wayahudi kwamba hawazishiki amri za mfalme, na mfalme akiona vyema andike barua waangamizwe, naye atalipa talanta 10,000 za fedha zake ili shughuli hii ifanyike. Mfalme akakubali asijue hila za Hamani, makamu wake; akavua pete yake, kama muhuri kuafiki alichosema Hamani na kumwambia, "fanya uonavyo vyema." Barua zikaandikwa ili kutimiza uovu huu kutoka katika ofisi ya mfalme, na kupelekwa kwenye majimbo kwamba Wayahudi wauawe na pia mali zao zichukuliwe nyara, matarishi wakatoka na kutangaza amri ya mfalme. Mfalme na Hamani wakakaa wanywe divai, lakini mji wa Shushani uliokuwa na Wayahudi wengi ukafadhaika. Huu ulikuwa mwaka wa sita toka Esta awe malkia, na mpaka wakati ule mfalme alikuwa hajui kwamba mke wake ni Myahudi!

*Waombee Wengine Katika Ombi la faragha—Katika ombi la faragha wote wana fursa ya kuomba kadri wapendavyo na kuwa wazi wapendavyo. Wanaweza kuomba kwa ajili ya jamaa na marafiki zao wote. Chumbani ni mahali pa kueleza shida zao zote binafsi, na mitihani, na majaribu. Mkutano wa pamoja wa kumwabudu MUNGU si mahali pa kufungua mambo binafsi au siri za moyoni.

---

Vashti alikataa kufanya nini? Nani walitaka kumwua mfalme Ahasuero? Kwa nini Hamani alimchukia Mordekai? Kwa nini Ahasuero hakujua kuwa mkewe ni Myahudi? Tabia zako bora ni zipi? Wazazi, walimu na walezi wako walikulea vipi katika maisha yako? Na unawezaje kuwaambukiza wengine nguvu hizi za tabia kama za Kristo kwa wengine pia?

**SIKU YA 157**
**(Juni 5)**

# Esta na Wayahudi Wafanya Maombi Maalumu

**-Esta 4-7**

Mordekai aliposikia hila za Hamani kuwaua Wayahudi wote alirarua nguo zake, akajivika magunia na kuweka majivu. Akatoka na kulia kwa uchungu, na katika himaya yote ambako amri ya mfalme na mbiu ilifika, palikuwa na msiba mkuu kwa Wayahudi na kufunga, na kulia na kuomboleza. Wengi wakalala juu ya magunia na majivu. Wajakazi wa Esta wakamjia na kumwambia habari hizo. Naye Malkia Esta alihuzunika na akampelekea Mordekai mavazi ili aondoe magunia yake lakini alikataa. Mordekai alimweleza Esta yaliyokusudiwa kwa Wayahudi, akamsihi aingie kwa mfalme, kumsihi na kuwaombea watu wake. Esta alijibu na kumkumbusha kwamba hakuna mtu yeyote, mwanamume au mwanamke anayeruhusiwa kumjia mfalme katika ua wa ndani bila kuitwa. Sheria ni moja tu, auawe, isipokuwa kama mfalme amemnyoshea fimbo ya dhahabu ili aishi. Esta akasisitiza, "wala mimi sikuitwa niingie kwa mfalme yapata siku thelathini." Mordekai akapeleka ujumbe wa dharura kwa Esta na kumwambia, "Wewe usijidhanie kuwa utaokoka nyumbani mwa mfalme, zaidi ya Wayahudi wote. Kwa maana wewe ukinyamaza kabisa wakati huu, ndipo kutakapowatokea Wayahudi msaada na wokovu kwa njia nyingine; ila wewe utaangamia pamoja na mlango wote wa baba yako; walakini ni nani ajuaye kama wewe hukuujia ufalme kwa ajili ya wakati kama huo?" Basi Esta akatuma ujumbe kwa Mordekai awakusanye Wayahudi wafunge kwa ajili yake wasile, wala kunywa kwa siku tatu.

Akasema, "nami na wajakazi wangu tutafunga vile vile; kisha nitaingia kwa mfalme, kinyume cha sheria, nami nikiangamia na niangamie." Mordekai akafanya kama Esta alivyomwambia. Siku ya tatu ilipofika Esta alijivika mavazi mazuri ya kifalme na kusimama katika ua wa ndani wa nyumba ya mfalme. Mfalme alikuwa ameketi juu ya kiti cha enzi na alipomwona Esta, akapata kibali machoni pake na mfalme akanyosha fimbo ya dhahabu kwake. Esta alikaribia na kuishika ncha ya ile fimbo. Mfalme akauliza haja yake ni nini naye atapewa hata nusu ya ufalme wake. Malkia Esta akamsihi mfalme aje kwenye karamu aliyomwandalia, yeye na Hamani. Mfalme alikubali ombi la malkia mara moja. Wakafika na kula na kunywa, mfalme akamwuliza Esta, "Dua yako ni nini? Nawe utapewa; haja yako ni nini?" Esta akasema kama amepata kibali machoni pa mfalme, mfalme na aje tena kwenye karamu aliyowaandalia kesho yake. Mfalme alikubali tena.

Hamani alifurahi sana kwa vile alikuwa amepata wadhifa na pia ni yeye peke yake aliyealikwa na mfalme kuhudhuria karamu kwa malkia. Lakini alipotoka na kumwona Mordekai hamwinamii, alikasirika sana ila akajizuia, akijipa moyo kwamba siku ya Wayahudi inakuja na wote wataangamizwa. Aliita marafiki zake na mke wake Zereshi na kuwasimulia habari za fahari, mali yake na watoto wengi alio nao, na pia mfalme alivyompandisha cheo kuwa makamu wake.

Akajisifu kuwa malkia alimwalika yeye tu kwenye karamu ya mfalme. Akasema, "yote yanifaa nini, pindi nimwonapo Mordekai." Mtu huyu mwenye cheo na mali alikuwa amejiharibia furaha yake kwa chuki, kwa mtu ambaye alimshinda uwezo. Ilikuwa kama aliyekunywa sumu na kutegemea kuwa ni mtu mwingine atayekufa. Mke na marafiki zake wakampa ushauri mbaya, kwamba "ufanyizwe mti wa mikono hamsini urefu wake … na useme na mfalme ili Mordekai atundikwe juu yake, ndipo utakapoingia kwa kicheko pamoja na mfalme karamuni."

Usiku ule mfalme akakosa usingizi na akaamuru kitabu cha kumbukumbu kiletwe, na hapo aliona kuwa Mordekai alimwokoa maisha yake wakati walinzi wake walipotaka kumwua. Akauliza, "Je! Ni heshima gani au jaha gani Mordekai aliyofanyiziwa kwa ajili ya hayo? Watumwa wa mfalme waliomhudumu wakamwambia, Hakuna alilofanyiziwa. Mfalme akasema, Yupo nani behewani? Ikawa Hamani alikuwa ameingia katika ua wa nje wa nyumba ya mfalme, aseme na mfalme, ili kumtundika Mordekai juu ya mti ule aliomwekea tayari. Basi watumwa wa mfalme wakamwambia, Tazama, Hamani yupo, amesimama behewani. Mfalme akasema na aingie. … Mfalme akamwuliza kwa kumshutukiza, "Afanyiziwe nini yule ambaye mfalme apenda kumheshimu?" Hamani, mtu mwenye 'umimi' akafikiri ni yeye, "Hamani akasema moyoni mwake, Ni nani ambaye mfalme apenda kumheshimu kuliko mimi? Basi Hamani akamwambia mfalme, Yule ambaye mfalme apenda kumheshimu, na aletewe mavazi ya kifalme ambayo mfalme amezoea kuyavaa, na farasi ambaye mfalme humpanda mwenyewe, ambaye ametiwa taji ya kifalme kichwani; na yale mavazi na yule farasi akabidhiwe mkononi mmojawapo wa maakida wa mfalme aliye mstahiki; ili makusudi amvike yule ambaye mfalme apenda kumheshimu, na kumkaribisha juu ya farasi kuipitia njia kuu ya mjini, na kupiga mbiu mbele yake, kusema, Hivyo ndivyo atakavyofanyiziwa mtu yule ambaye mfalme apenda kumheshimu. Basi mfalme akamwambia Hamani, 'Hima! Twaa mavazi na farasi kama ulivyosema, ukamfanyizie vivyo hivyo Mordekai, Myahudi, aketiye mlangoni pa mfalme; lisipungue neno lolote katika yote uliyoyasema." Je! waweza kupiga picha jinsi uso wa Hamani ulivyokasirika wakati akimpa Mordekai heshima hii. Alifika nyumbani kwake na kuwaeleza mke na rafiki yake yale yaliyompata. Mkewe akamwambia, kama huyu Mordekai ambaye umeshaanza kumsujudia ni Myahudi, hutamweza, bali kuanguka utaanguka mbele yake. Mama huyu alikuwa si nabii ila alipewa hekima ya kuona mbali. Wakiwa bado wanazungumza, watumishi wakaja kumchukua Hamani kwa karamu ya mfalme. Walipokuwa wakiendelea karamuni, mfalme alimwuliza malkia tena, "Dua yako ni nini? Nawe utapewa, na haja yako ni nini?" Esta akasema, "Ikiwa nimepata kibali machoni pako…nipewe maisha yangu kuwa dua yangu, na watu wangu kuwa haja yangu."

Esta akamweleza mfalme hila za Hamani kumwua na watu wake, na kwamba hata binamu yake Mordekai ambaye ni kama baba yake anachukiwa sana na Hamani. Akasema kama wangeuzwa kuwa watumwa angalinyamaza, ila ni kuuawa. Mfalme akauliza ni nani anataka kumwua na watu wake, akajibu "ni mtesi, tena ni adui, huyu hapa Hamani, mtu mbaya kabisa." Hamani akaingiwa na hofu. Mfalme akasimama kwa ghadhabu kwenda kwenye bustani yake. Hamani naye akasimama apige magoti kwa Esta maana alijua amekusudiwa madhara. Mfalme aliporudi

akamwona Hamani amejitupa chini penye kitanda alipokuwa Esta, mfalme akasema, “Namna gani! Je! Atamfanyia malkia jeuri hata machoni pangu nyumbani mwangu? Watumishi wakamfunika uso Hamani kumaanisha kuwa atauawa saa yoyote. Ndipo mfalme akaelezwa juu ya ule mti aliotengeneza Hamani ili kumtundika Mordekai nyumbani kwake, mfalme akageuza na kusema “mtundikeni Hamani juu yake.” Basi Hamani akatundikwa kwenye mti wa futi 86, na hivyo shimo alilochimba waingie wengine aliingia mwenyewe. Tunapowatakia wengine maovu, uovu huo unaweza kuturudia sisi wenyewe. Kuwatakia watu wa Mungu maovu ni jambo baya zaidi, hata wakikufanyia vibaya, mwache Mungu akulipie kisasi. Kwa nini tunapaswa kusikiliza mashauri kutoka kwa Mungu? “Mungu si mwanadamu, hata aseme uongo.”— Hesabu 23:19.

Esta aliomba na kufunga na wenzake, na tunaona tofauti iliyoletwa. Baba yetu wa mbinguni anangoja kutupa utimilifu wa baraka Zake. Ni fursa yetu kunywa kwa kiasi kikubwa kwenye chemchemi ya upendo usio na mipaka. Inashangaza sana kwamba tunaomba kidogo sana! MUNGU ameridhia na Yuko tayari kusikia maombi ya dhati ya aliye mnyenyekevu zaidi kati ya watoto Wake, na bado kuna kusitasita kwa wazi kwa upande wetu kumjulisha MUNGU mahitaji yetu. Malaika wa mbinguni wanaweza kufikiria nini juu ya wanadamu dhaifu wasiojiweza, ambao wako chini ya majaribu, wakati moyo wa MUNGU wa upendo usio na kikomo unawahitaji, tayari kuwapa zaidi ya wanavyoweza kuomba au kufikiria, na bado wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo?

*Wakati vijana wanapoenda kuhubiri Ukweli, mnapaswa kuwa na majira ya maombi kwa ajili yao. Omba kwamba MUNGU awaunganishe na Yeye Mwenyewe na awape hekima, neema, na maarifa. Ombeni ili waweze kulindwa na mitego ya Shetani iliyojificha na kuwekwa safi katika mawazo na utakatifu wa moyo. Ninawasihi ninyi mnaomcha Bwana, msipoteze wakati katika mazungumzo yasiyofaa, au katika kazi isiyo na maana, ili kujipatia kiburi, au kuridhisha tamaa ya chakula au ya mwili. Hebu wakati unaopatikana utumike katika kupambana mieleka na MUNGU kwa ajili ya wachungaji/wahudumu wenu. Inueni mikono yao kama Haruni na Huri walivyoifanya mikono ya Musa.

---

Mfalme alionyeshaje shukurani yake kwa Mordekai? Mti aliotengeneza Hamani ili kumtundika Mordekai ulitumiwaje? Kwa nini Esta alifunga? Kwa nini ni dhambi kuwatakia watu maovu? Kupotelewa usingizi waweza kuwa muda mzuri wa kuomba, mfalme alifanya nini alipokosa usingizi?

**SIKU YA 158**
**(Juni 6)**

# Mordekai Apandishwa Cheo na Wayahudi Wajitetea

**- Esta 8-10**



Siku ile mfalme alimpa Esta nyumba ya Hamani. Esta alimwambia mfalme juu ya uhusiano wake na Mordekai, hivyo akaja mbele ya mfalme. Mfalme akaivua pete aliyompokonya Hamani akampa Mordekai, ikimaanisha kuwa alichukua nafasi ya Hamani ya kuwa waziri mkuu au makamu wa mfalme. Esta akaanguka miguuni pa mfalme, akamsihi na kumkumbusha kwamba barua zilishapelekwa za kuwaua Wayahudi, na kama sheria za Wamedi na Waajemi zilivyo, haziwezi kubadilika, kwa hiyo kuuawa kwa Wayahudi ni hakika bado kupo. Akaomba mfalme atangue zile barua ili mabaya yasiwajie Wayahudi, ambao ni malkia na jamaa zake malkia. Mfalme akamwambia kwamba amempa mamlaka, yeye aandike tu kufuta uovu kwa Wayahudi naye ataweka muhuri kwa pete ya mfalme. Waandishi wa mfalme wakaitwa na barua kuandikwa majimbo yote waliyoyatawala kuanzia Ulaya, Asia na Afrika. Barua iliwaruhusu Wayahudi wakusanyike na kujihami maisha yao na mali zaoa ili wasiangamizwe, yaani, wajilipize kisasi juu ya adui zao. Matarishi waliondoka na ujumbe ili kuupeleka katika majimbo yote, wamepanda wanyama wepesi sana waliotumika kwa huduma za mfalme, na kupiga mbiu huko Shushani ngomeni. Mordekai naye akatoka amevaa mavazi ya kifalme na taji kubwa ya dhahabu, mji wa Shushani wakashangilia, ikawa nuru, shangwe, furaha na heshima

kwa Wayahudi. Hata siku hiyo watu wengi wakajifanya Wayahudi maana walipata hofu kwamba maovu au chuki waliyotaka kuwafanyia itawarudia.

Basi ikawadia siku ya Wayahudi kuuawa, lakini amri ya pili ya mfalme ilisema wanaweza kujitetea. Ndipo watu wasio Wayahudi waliingiwa na hofu ajabu, maana sasa walijua malkia na makamu wa mfalme ni Wayahudi! Sifa za Mordekai zikavuma, kwani alikuwa mcha Mungu na mwenye hekima. Wayahudi wakapiga maadui zao kwa maangamizo makubwa, wakawatenda kama wapendavyo wale waliowachukia. Wakauawa watu 500 Shushani na wana kumi wa Hamani. Mfalme akaletewa hesabu, na akawaambia Wayahudi lolote waombalo watapata. Basi wakaruhusiwa tena kufanya vilevile siku iliyofuata na hata kuwatundika wana kumi wa Hamani kwenye miti, basi wakaua watu wengine siku ile, jumla ikawa watu 75,000 waliouawa. Ila hawakuchukua vitu vyao au nyara zozote. Lilikuwa jambo la kusikitisha sana, kwamba uovu wa mtu mmoja, mbinafsi, uliweza kuleta mauti na uchungu mwingi, hata kwa wale wasiohusika. Mara nyingine ukisikia mtu anafanya uovu, usijiunge naye na uwe tayari kumshauri kuacha, maana ni nani ajuaye kama "hukujia nafasi hiyo kwa ajili ya wakati kama huo?" Maana ukinyamaza, waweza kuwa miongoni mwa watakaoumizwa badala ya wale unaofikiria.

Basi Wayahudi walipumzika na kufanya karamu ya furaha, na kupelekeana zawadi. Mordekai akawaandikia watu kwamba siku hiyo waishike Wayahudi, kwani walijipatia raha mbele ya adui zao, badala ya huzuni ikawa furaha, wakaiita sikukuu hii Purimu au kupiga kura. Yote haya yalitokea kwa sababu Hamani Mwagagi, aliyejitwika ujinga kwa kuwa adui wa Wayahudi bila sababu yoyote, mambo yalimrudia mwenyewe. Tunapaswa kuushinda ubaya kwa wema. Wayahudi wakaagiza watu washike siku hii na wazao wao ili ikumbukwe vizazi vyote, na Purimu isikome kuadhimishwa.

Mfalme Ahasuero akatoza kodi katika nchi, visiwa na bahari, na matendo yake ya nguvu na ushujaa na ukuu yakajulikana pote. Hata Mordekai akapewa ukuu, na haya yote yakaandikwa kwenye taarifa ya kitabu cha wafalme wa Umedi na Uajemi, naye akaendelea kuwafanyia watu wema.

Maana ya Esta ni nyota, alikuwa nyota kwa watu wake na kuwaokoa. Ni kweli alikuwa na uzuri wa sura, lakini zaidi, ni kwamba Mungu alimchagua aonekane uzuri wake mbele ya watu ili awaokoe watu Wake, naam, kizazi cha masihi. Hata leo, Mungu ana mpango maalumu nawe ili usiangamie. Muombe na umwulize, akwambie mipango aliyo nayo kwako kupitia Neno lake. Basi Esta hakuwa na papara, akasirike na kumwambia mfalme, kwa haraka yote ambayo Hamani alitaka kuwatendea Wayahudi, bali aliendа taratibu kwa hekima. Hata wajakazi wake walikuwa tayari kufunga pamoja naye, maana walimpenda, kama angekuwa mbaya kwa wajakazi wake, wangefikiri ni bora afe tu. Esta alisaidia kazi ya Ezra na Nehemia, maana mume wake aliwafanyia Wayahudi mengi mazuri kwa ajili ya Esta. Hata mbiu ya mwaka 457 KK ya Wayahudi ya kurudi Yerusalemu ilitolewa na mume wake. Mungu aliwabariki wafalme hawa, kuanzia Dario, Koreshi, Ahasuero kuwa wema kwa Wayahudi baada ya Wakaldayo kuwaumiza vibaya. Waliruhusu Wayahudi waabudu na kufanya shughuli zao. Nehemia na Ezra walipata kazi nzuri

kwa mfalme wakati huu. Tukumbuke kwamba Maandiko yanasema kuwa Wakaldayo walipewa ruhusa na Mungu kuwaadhibu Wayahudi kwa uovu wao wa kuasi sheria ya Mungu na kuabudu miungu mingine. Walizivunja Sabato zake. Sabato hizi ni pamoja na zile za Yubile za kuachia wafungwa mwaka wa 50, au kuacha kutolima mwaka wa saba ili maskini wawe na chakula. Pale tu tunapojali haja zetu, tusijali maskini na wenye mahitaji, tutajiletea maumivu mengi.

Hamani alinuia uovu, kwa ajili ya kumchukia mtu mmoja alitaka aue maelfu ya watu. Hata hivyo, Mungu alikuwa amepanga toka zamani kuokoa watu wake kwa kufanya Esta achaguliwe kuwa malkia, na Mordekai amsaidie Esta.
Ukiyatafakari maisha ya Hamani, jiulize leo, Je, mimi napanda mbegu gani chungu kwa watu wengine, Je, hasira na kiburi vinakaa moyoni mwangu? Tumwombe Mungu aziondolee mbali, na apande mbegu Zake za wema na kuheshimiana na wengine moyoni mwangu, ili tuweze kuonyesha upendo Wake kwa wengine. Ubinafsi na kiburi huumiza na kuharibu, lakini wema, ukarimu na fadhila, huponya wengine na kuwaletea matumaini. Ni mahusiano gani maishani mwako yanahitaji uponyaji, na utawaponyaje kwa wema na ukarimu wengine? Ni magumu gani makubwa maishani mwako ambayo wewe kama Esta, utakabiliana nayo kwa ujasiri zaidi kwa msaada wa marafiki wanaosali kwa niaba yako?

*Nguvu ambayo haijawahi kuonekana hapo awali inamiliki ulimwengu. Katika maburudisho, katika kutafuta pesa, katika kugombea madaraka, katika mapambano ya kuishi, kuna nguvu ya kutisha ambayo huchota mwili na akili na roho. Katikati ya msukumo huu unaovuruga, MUNGU anazungumza. Anatuamuru tujitenge mahali pa faragha na tuzungumze Naye. "Nyamazeni, mjue ya kuwa Mimi ni MUNGU." Zaburi 46:10.

---

Wayahudi walijiteteaje? Kwa nini Wayahudi walichukuliwa utumwani? Wayahudi ina maana gani? Jina jingine la Esta lilikuwa nani? Mordekai alipewa cheo gani? Purimu ilikuwa sikukuu gani? Tunapobariki wengine nasi tunabarikiwa, je, umeliona hili maishani mwako? Mfalme alionyeshaje shukurani yake?

**SURA YA 159**
**(Juni 7)**

# Mtu wa Mungu Ayubu

Siku kabla ya Musa, palikuwa na mtu katika nchi ya Usi. Musa anasemekana kuwa ndiye aliyeandika kitabu cha Ayubu. Kitabu hichi kiliandikwa baada ya kitabu cha Mwanzo. Mtu huyu alikuwa mkamilifu, mwelekevu, na aliyemcha Mungu akiepukana na uovu. Alikuwa na wana saba na mabinti watatu. Alikuwa na kondoo 7000, ngamia 3000, ngombe 1000, na punda 500. Watu wa nyumbani mwake walikuwa wengi sana. Ayubu alikuwa tajiri na mwenye kuheshimiwa na watu. Alitoa kafara kwa ajili ya watoto wake kila siku akisema, "Yumkini hawa wanangu wamefanya dhambi, na kumkufuru Mungu mioyoni mwao." Ndivyo alivyofanya Ayubu siku zote.

Ilikuwa siku moja wana wa Mungu walikwenda kujihudhurisha mbele za Bwana, Shetani naye akaenda kati yao. BWANA akamwuliza Shetani "umetoka wapi?" Naye akajibu, "natoka kuzunguka-zunguka duniani, na katika kutembea huku na huku humo." BWANA akamwuliza, "Je! Umemwona mtumishi Wangu Ayubu? Kwa kuwa hapana mmoja aliye kama yeye duniani, mtu mkamilifu na mwelekevu, mwenye kumcha Mungu na kuepukana na uovu." Shetani akasema kumbe hujui, ni kwa vile umemwacha bila shida, yaani, umemzingira kwa wigo pande zote, familia yake na vitu vyake vyote. Kazi za mikono yake umezibarikia, nayo mali yake imeongezeka katika nchi. Lakini nyosha mkono wako sasa, uyaguse hayo yote aliyo nayo, naye atakukufuru mbele za uso wako." Bwana akamruhusu Shetani kwamba afanye lolote kwa Ayubu ila asichukue uhai wake. Na Shetani akatoka mbele za uso wa Bwana.

Ilitukia siku moja watoto wa Ayubu walikuwa wakila na kunywa divai katika nyumba ya ndugu yao mkubwa, mjumbe akamfikilia Ayubu na kumwambia, Hao ng'ombe walikuwa wakilima na punda walikuwa wakilisha karibu nao, mara Waseba wakawashambulia, wakawachukua wakaenda nao, wamewaua hao watumishi kwa makali ya upanga. "Mimi peke yangu nimepona, mimi tu, kukuletea habari." Kisha mwingine akaleta ujumbe kwamba moto umetoka kwa Mungu na kuteketeza kondoo na watumishi wanaowachunga, "mimi peke yangu nimepona, mimi tu kukuletea habari." Huyo alipokuwa akali akinena, akaja mjumbe mwingine na kusema, Wakaldayo walifanya vikosi vitatu wakaja na kuwachukua ngamia na kuwaua watumishi kwa upanga na "mimi peke yangu nimepona, mimi tu, kukuletea habari." Ndipo wa mwisho akaja na kusema, watoto wako walipokuwa kwa ndugu yao wakila na kunywa divai, upepo wenye nguvu kutoka jangwani ulikuja na kuipiga nyumba kwa pembe zake nne nayo ikawaangukia hao vijana, nao wamekufa, "mimi peke yangu nimepona, mimi tu, kukuletea habari." Ndipo Ayubu akainuka, akalirarua joho lake, akanyoa kichwa chake, na kuanguka chini, na kusujudia. Akasema "Mimi nilitoka tumboni mwa mama yangu nili uchi, nami nitarudi tena huko uchi vile vile. BWANA alitoa na BWANA ametwaa; Jina la BWANA na libarikiwe."

Katika mambo hayo yote Ayubu hakufanya dhambi, wala hakumwazia Mungu kwa upumbavu.

Basi siku nyingine tena, wana wa Mungu wakaenda kujihudhurisha mbele za BWANA, Shetani naye akaenda kati yao. BWANA akamwuliza Shetani, "Umetoka wapi?" Akajibu tena kuwa anatoka kuzunguka-zunguka duniani, na kutembea huku na huku humo. Naye BWANA akajisifia mtu Wake Ayubu kwamba ni mwaminifu, wala hapana kama yeye duniani. Kweli Ayubu alikuwa na sifa nzuri, nasi watoto tukazane ili kwa neema yake, Mungu ajisifie kuwa sisi ni watu Wake. Basi BWANA akaeleza mema ya Ayubu na kumwambia Shetani japokuwa "ulinichochea juu yake ili nimwangamize pasipokuwa na sababu." Shetani akamjibu na kusema, "ngozi kwa ngozi," yaani, Mungu aruhusu mwili wake Ayubu upate shida. Shetani akasema, "lakini sasa nyosha mkono wako, uuguse mfupa wake na nyama yake, naye atakukufuru mbele za uso wako." BWANA akamruhusu Shetani kumjaribu Ayubu katika mwili wake. Akampiga Ayubu na majipu mabaya tangu wayo wa mguu mpaka utosini. Ayubu akashika kigae cha kujikunia akaketi majivuni, kisha mke wake akaja na kumwongezea maumivu kwa kumwambia "Je! Wewe hata sasa washikamana na utimilifu wako? Umkufuru Mungu ukafe." Naye Ayubu akamwambia "Wewe wanena kama mmoja wa hao wanawake wapumbavu anenavyo. Je! Tupate mema mkononi mwa Mungu, nasi tusipate na mabaya?" Katika mambo hayo yote Ayubu hakufanya dhambi kwa midono yake.



Marafiki watatu wa Ayubu, yaani, Elifazi, Bildadi, na Sofari waliposikia habari mbaya zilizompata, wakaja ili wamtulize moyo. Walipomtazama, hawakuweza kumtambua, wakainua sauti zao na kulia, kila mmoja akararua joho lake, wakarusha mavumbi juu ya vichwa vyao kuelekea mbinguni. Wakaketi kwa siku saba bila kunena naye neno lolote, kwani waliona kuwa mashaka yake ni makuu mno. Ndipo Ayubu akafungua kinywa chake na kuilaani siku aliyozaliwa, akisema ingelikuwa

bora kama asingezaliwa. Siku hizo watu waliamini kwamba watu wote waliopata shida, magonjwa au kifo, ilikuwa ni kwa sababu Mungu alikuwa amewakasirikia na ni wenye dhambi mno. Watu hawa hawakuwa wameelewa kuhusu vita au pambano kati ya Mungu na Shetani au wema na ubaya iliyoanzia kule mbinguni. Na kwamba hata walio wema hupata maumivu na shida nyingi. Marafiki hawa watatu walitoa hotuba ndefu kwa Ayubu. Walikazana kumwambia Ayubu aungame, kwani shida zile nzito zimetokana na dhambi zake. Ayubu akasema hakufanya lolote baya na kwamba alijitahidi sana kutenda mema, ila hakujua kwa nini maafa ya namna ile yalimfika. Ayubu alishangaa imekuwaje Mungu ameacha mateso na shida zile zote zimpate kiasi kile. Ayubu hakuelewa njia za Mungu, au kwamba Shetani alijadiliana Naye. Yeye aliamini kuwa Mungu ni mwema na alimtegemea kabisa. Alisema, "Lakini najua ya kuwa mteteaji wangu Yu hai, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi … na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, lakini…nitamwona Mungu… macho yangu yatamtazama, wala si mwingine." Kijana Elihu alikuja baadaye, naye alinyamaza kwanza maana wengine walikuwa wakubwa kwake, baadaye akasema alitaka kuwa msaada tu kwa Ayubu, na siyo kumshinikiza Ayubu aungame.

Mwisho, Mungu mwenyewe alizungumza, akasema, "Basi jifunge viuno kama mwanamume, maana nitakuuliza Neno, nawe niambie… Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi? Haya! Sema kama ukiwa na ufahamu…" (soma Ayubu 38-42). BWANA aliwaambia wale marafiki watatu waungame, kwani hawakuwa na haki au maarifa ya kumhukumu Ayubu. Mungu Ndiye mhukumu na anafanya haki kwa kila mtu. Aliwaambia watoe kafara ya kuomba msamaha, na Ayubu awaombee ili wasamehewe. Ayubu aliwaombea rafiki zake na Mungu aliwasamehe, kwa sababu ya uaminifu wa Ayubu. Ayubu naye akaungama kwa Mungu kwani aliona hakuelewa, lakini sasa alipata uhakika kuwa anapendwa sana. Mungu akampa Ayubu maradufu ya ngombe, kondoo ngamia, punda na vyote alivyokuwa navyo. Mungu akampa tena Ayubu watoto kumi, wavulana saba na wasichana watatu. Wasichana hawa warembo waliitwa Yemima, Kezia na Keren-hapuhu. Baada ya shida zile Ayubu aliishi miaka mingi akiwa na mali, heshima na wema kwa watu na kufurahia ulinzi wa BWANA.

Kitabu cha Ayubu kama tulivyosema, kilikuwa kitabu cha kwanza kuandikwa na Musa nacho kimetupa picha ya Pambano kuu kati ya wema na uovu. Swali limeulizwa kwa mahakama ya mbinguni kuhusu haki na upendo wa Mungu (Theodicy) * Theodisi ni neno la Kigiriki. Theodisi ni jaribio la kumtetea Mungu kuhusiana na uovu unaoendelea kwa kujibu tatizo lifuatalo: kama Mungu ni mwema na mwenye nguvu zote na kwa hivyo, Yeye anajua yote, kwanini basi anaruhusu kuwe na mateso duniani namna hii? Sisi Hatutajidai kwamba tunajua habari zote katika kulijibu swali hili, kwani ni Mwenyezi Mungu tu Ndiye anayejua yote, ila kutokana na Maandiko Matakatifu, tunaona kupitia kwenye dirisha dogo sababu za Mungu kuruhusu mambo fulani kutokea au kuendelea kuwepo, na anawekaje mipaka na huku akizifuata sheria za pambano kuu linaloendelea kati ya wema na ubaya, kati Yake na Shetani.

Upendo wa Mungu unatusaidia kidogo kuelewa kwa nini MUNGU anaruhusu mambo fulani kutokea pamoja na mapungufu anayoyazingatia anapotafuta

kufuata sheria za vita kati yake na Shetani. Sheria hizi hazina lebo ila tabia ya Mungu imeshitakiwa na kupakwa uchafu kuhusiana na Upendo na haki Yake. Watu huuliza kwanini mabaya hutokea wakati Mungu ni mwema. Tunajua kwamba Mungu amewapa viumbe Wake uhuru, nao wanaweza kuutumia uhuru huo kufanya mambo wanayopenda. Na hilo likaleta mateso binafsi, au kwa watu wengine wanaomzunguka. Jambo jingine nililoliona ni furaha ya malaika baada ya uumbaji.

Ila tunagundua kwamba mengine mateso mengine hayahusu uchaguzi wa binadamu, kama vile majanga ya asili n.k. Na tunaweza kuuliza basi kwanini Mungu asiyazuie hayo majanga, au kwanini Mungu asiwaonye watu kuhama, hapa ndiyo tunagundua kwamba si binadamu peke yake anayehusika katika mateso au uovu unaotendekea, kuna mambo ya kina zaidi. Shetani pia ni kiumbe aliyepewa uhuru, naye ana maabara yake ya uovu. Mungu huwa hapati kutenda kile angependa kutenda mara zote, au hapati anachotaka wakati wote. Jambo hili huwa linatushangaza kwa vile tunajua Mungu ana nguvu na uwezo wote na hivyo tunafikiri kwamba daima Yeye hupata anachokitaka! Tunaona mara nyingi kwenye Maandiko Mungu akiomboleza, mfano Zaburi 81 anamwambia mwanadamu amgeukie Yeye, "Nami nitakuokoa" au Marko 6 yasema Yesu alipokuwa Nazareti hakuweza kufanya miujiza kule kwasababu ya kule kutoamini kwao. Yaonekana hapa uweza wa Mungu ulizuiliwa kwaajili ya imani ndogo. Danieli 9 na 10 yasema Danieli ilikuwa ajibiwe maombi yake, ila kulikuwa na ucheleweshо wa wiki tatu kwaajili ya mfalme wa Uajemi, ambaye alimwakilisha Shetani. Kufa kwa Yohana Mbatizaji, kwaonekana ni jambo ambalo adui alilifanya pia na Yesu hakuweza kutenda jambo kwasababu tusizozijua.

Wanafunzi waliposhindwa kumponya mtoto aliyeletwa na babaye, Yesu alisema pepo hili haliwezi kutolewa isipokuwa kwa maombi na kufunga. Na baba mtoto akasema, Bwana naamini, nisaidie kutoamini kwangu! Basi tunaona maombi, na kufunga, na uchaguzi wetu unachangia yale yanayoendelea kwenye pambano duniani. Ila ufalme wa giza pia unachangia kitu.

Yesu ameona ili kuurudisha ulimwengu Kwake hawezi kutumia uwezo au nguvu Zake ila upendo! Sheria za vita lazima ziwepo, Naye amehusika kuziweka, isipokuwa ameweka ahadi au mipaka ya kuthibiti mambo fulani na Mungu anatunza ahadi Zake mfano katika 2 Mambo ya Nyakati 7:14 inaonyesha watu wakitokomea kwenye uovu, kuna mambo yanayoweza kuwarudisha. Ulimwengu umejiuza wenyewe kwenye nguvu za mapepo, na Mungu anaurudisha kupitia upendo Wake. Hawezi kutumia nguvu. Kwani hatuwezi kumpenda kama atatenda kwa jeuri. Hatuwezi kuwa karibu na Yule ambaye hatuwezi kumuamini, itatuletea hofu ya kumtii.

Nani anateseka zaidi basi? Hakika ni Mungu. Lakini siku moja atakomesha mateso, na dhambi haitainuka tena kamwe Nahumu 1:9. Hatayakatishwa kabla ya watu kuona picha halisi ya jinsi Shetani alivyo, lakini baada ya maswali ya watu kujibiwa mioyoni mwao. Kitabu cha Ayubu na vinginevyo vinatupa picha ya Korti kwenye nyua za mbinguni. Mungu hawezi kutumia nguvu au kulazimisha watu kujibu tuhuma anazotupiwa na Shetani, kwani ataonekana ana hatia ya mateso yanayoendelea duniani. Pia hawezi kuyazima mashitaka. Mungu anashugulikia hoja

alizotuhumiwa kulingana na sheria za pambano (engagement rules), adui ameweka mipaka kwenye maamuzi ya kisheria. Nasi hatujui kile Mungu anachokijua. Tunaona shamba lilipandwa vyema ila magugu yakatokezea, Mwenye shamba ni Mwana wa Adamu, ila tunagundua adui ndiyo ametenda hivyo, yaani amepanda magugu- Mathayo 13. Hakika mambo haya ni magumu sisi kuyajua kwa uhalisi. Ila tutulie katika hekima Yake, nasi siku moja tutaelezea kila kitu, kwa sasa ulimwengu wetu u katika tamasha. 1 Wakorintho 4:9. Ukipata kitabu kinaitwa Pambano kuu tafadhali kisome hicho kitakupa picha kubwa zaidi, kama huna tutakutumia mtandaoni. Dr John Peckham ameandika kitabu kizuri kikipembua pambano hili kubwa lililoanza mbinguni na linalokaribia kuisha katika kitabu kinachoitwa Theodicy of Love. Nashauri watu wenye kukipata wakisome, na pia ana video kadhaamtandaoni kwa jina lake kwenye youtube.

Maneno haya yalete furaha kwetu leo, kwani siku moja tutayatamka kule mbinguni! "Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia vikisema: Baraka na heshima na utukufu na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na Yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele." Ufunuo 5:13.

Pambano lile kuu limeisha. Dhambi na wenye dhambi hawapo tena. Malimwengu yote ni safi. Kishindo kimoja tu cha maelewano na furaha ndicho kinachogonga katika uumbaji Wake wote ulio mpana sana. Kutoka Kwake Yeye aliyeviumba vyote, hububujika uhai, uzima, nuru na furaha, katika ufalme Wake wote, katika anga na milki isiyo na kikomo au mipaka. Kuanzia kwenye ile chembe ndogo kabisa ya atomi hadi kwenye ulimwengu mkubwa zaidi, vitu vyote, vyenye uhai (vyenye seli) na visivyo na uhai (vyenye atomi), katika uzuri wao usiofunikwa na kivuli chochote na furaha yao iliyo kamilifu kabisa, vinatangaza kwamba MUNGU NI UPENDO. (1Yohana 4:8!). [PK 678.3]

Ufunuo 12 inachora drama ya vita huko Mbinguni. Mikaeli na malaika Zake wanapigana vita dhidi ya Shetani na malaika zake, na hakuna nafasi tena iliyopatikana kwa ajili ya malaika wa Shetani Mbinguni—walitupwa nje. Lakini Shetani alikuwa nani? na vita vya Ayubu vilihusu nini? Hilo ndilo Ayubu hakujua, ila sisi tumepata nafasi ya kujulishwa.

Sentensi inayosema "Hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, Na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha?". Jambo hili linanifanya nifikiri kwamba hisia za malaika si tofauti sana na zile tulizopewa wanadamu! Katika toba yake, je, Ayubu alitambua kwamba bado alikuwa na mengi ya kujifunza? Je, wewe bado unayo maswali mengi kuhusu Mungu? Basi ni Vyema! Una mapumziko ya umilele ambayo utapata muda wa kuuliza na kupata majibu! Lakini, Mungu bado ametupa majibu mengi kupitia mafunuo yake katika Maandiko ya Biblia na Roho ya Unabii.

OMBI: Mungu mpendwa,
Watu wengi wasio na hatia wanateseka na Wewe pekee Ndiye unajua kwanini. Lakini pia unajua kwamba hakuna kitu kinacholinganishwa na baraka na zawadi utakazotoa wakati wa kuja Kwako. Kwa hiyo tukumbuke katika ufalme Wako wa

neema. Amina.

*Wakati Ubinafsi unapokufa, kutakuwa na uamsho wa hamu kubwa kuhusiana na wokovu wa wengine, - matamanio ambayo yatasababisha juhudi za kudumu na zenye uvumilivu katika kutenda mema. Kutakuwa na kupanda kando ya maji yote; na dua ya dhati, zizochoka, maombi ya kudumu, yataingia mbinguni kwa ajili ya nafsi zinazoangamia.


---

Ayubu aliishi wapi? Mungu alimwuliza nini Shetani? Ayubu alisema nini wakati mambo mazito hivi yalipomtokea? Unafikiri Ayubu alijisikiaje marafiki walipotoa 'faraja' yao? Kwa nini kuhukumu watu si vizuri? Utatofautishaje kati ya kumwambia rafiki aache uovu na kumhukumu? Kwa nini hatimaye Mungu alimbariki Ayubu? Kwa kuuliza maswali hayo yote, je, Mungu alikuwa akimtia moyo Ayubu ili asikilize na kujifunza?

**SIKU YA 160**
**(Juni 8)**

# Danieli Aenda Uhamishoni

**- Danieli 1**



Kitabu cha Danieli kina maelezo mafupi ya historia, unabii wa wakati wake, na ule wa siku za usoni. Unabii huo unatujulisha kwamba sasa tupo wapi, na mwisho wa dunia ni lini. Hausemi siku wala saa, ila unatupatia ramani ya ukaribu wake, na kwamba tufanye nini? Danieli mwenyewe aliandika. Madhumuni makuu ya unabii ni kufunua Ahadi za Mungu, na siyo kufunua matukio ya siku zijazo. Tunapokita kwenye matukio, na utabiri wa mnyama na mengine, hayo ni mapitio tu katika kufunua tabia na upendo Mungu lakini siyo dhumuni lenyewe. Manabii walichunguza unabii kutafuta ahadi na si matukio. Tusifundishe unabii ambao hauleti maana, au tusimtafute Mungu bure "Kuhusu wokovu huo, manabii ambao walitabiri habari za neema itakayowafikia ninyi, walichunguza sana" 1 Petro 1:10, Tusiishie kuwa na ujuzi tu kwenye akili na tusifikie kwenye wokovu.

Kama tulivyoona huko nyuma, Danieli alikuwa miongoni mwa watu waliochukuliwa kwenda uhamishoni Babeli wakitokea Yuda. Hii ilikuwa miaka kama 600 KK. Mfalme alimwambia Ashpenazi, mkuu wa matowashi wake atwae baadhi ya vijana wa Israeli wa uzao wa kifalme na kiungwana, wasio na mawaa, wazuri wa uso, wajuzi wa hekima, werevu, wenye maarifa, wenye kufahamu elimu, watakaoweza kusimama katika jumba la mfalme. Akasema wafundishwe elimu na lugha ya Wakaldayo.

Mfalme akaagiza wapewe posho ya chakula alichokula na divai aliyokunywa. Akaagiza walishwe hivyo muda wa miaka mitatu, kisha wasimame mbele ya mfalme. Hata leo hivi tukiambiwa tukae na kula vyakula vya mfalme, tunajua vitakuwa vizuri na vya gharama, japokuwa vinaweza kuwa na madhara kwa afya.

Katika hawa walikuwapo baadhi ya wana wa Yuda, kwa majina ni Danieli, Hanania, Mishaeli na Azaria. Na mkuu wa matowashi akabadilisha majina yao, Danieli

akaitwa Belteshaza, Hanania akamwita Shadraka, Mishaeli akamwita Meshaki; na Azaria akamwita Abednego. Majina haya yalikuwa mabaya, kwa vile yalikuwa ya miungu ya Wakaldayo. Lakini Danieli aliazimu moyoni mwake ya kuwa hatajitia unajisi kwa chakula au divai ya mfalme. Akamsihi mkuu wa matowashi ampe ruhusa asijitie unajisi. Inawezekana chakula hiki kilitolewa kafara kwa miungu ya Wakaladayo, au walikula nyama najisi kama nguruwe, pweza, kamba, au vinginevyo. Mungu akamjalia Danieli kupata kibali na huruma machoni pa yule mkuu. Mkuu huyu akasema, "mimi namwogopa bwana wangu, mfalme, aliyeagiza chakula na vinywaji vyenu, asije kuona sura zenu na ngozi hazipendezi kama rika zenu, kisha nikahatarisha maisha yangu mbele ya mfalme." Ni kweli chakula tulacho, na mambo ya afya tufanyayo yanabariki afya zetu au kulaani. Mungu alitoa sheria za ulaji kwa watu katika Neno Lake. Hata siku hizi tusikae na kula ovyo kwa ulafi, eti chakula ni chakula tu. Dhambi iliingia kupitia kwa chakula, bustani ya Edeni ilipotea kwa ajili ya chakula.

Basi Danieli akamsihi yule mkuu awajaribu yeye na wenzake kwa siku kumi, akiwapa vyakula vya mimea kama mtama na maji, kisha awapime ili aone, naye akawasikiliza. Vyakula ambavyo vinaanza kuota vina nguvu kuliko vyakula vya kawaida kwa madini na vitamini, hivyo, mbegu kama mtama, jamii ya karanga, na jamii ya maharage, mboga na matunda, ndiyo vijana hawa walikula. Baada ya siku kumi walionekana nyuso zao zikiwa nzuri zaidi, miili yao ilinawiri zaidi, kuliko wale vijana waliokula chakula cha mfalme. Basi msimamizi akaondoa chakula na vinywaji vya mfalme akawapa vyakula hivi vya mimea tu na maji.

Mungu aliwapa hawa vijana maarifa na ujuzi katika elimu na hekima, na Danieli alipewa ufahamu katika maono yote na ndoto. Ikapita miaka mitatu aliyoagizwa, kisha wakasimama mbele ya mfalme Nebukadreza. Mfalme akazungumza nao na ikaonekana hakuna aliyekuwa kama wao katika jambo la hekima au ufahamu alilowauliza mfalme na akawaona walifaa mara kumi zaidi ya waganga, na wachawi wa ufalme wake. Danieli aliendelea kufanya kazi katika ofisi ya mfalme mpaka mwaka kwa kwanza wa Koreshi, mfalme wa Uajemi. Hii ni huduma ya zaidi ya miaka 70 kwani Wakaldayo walitawala miaka sabini kabla ya Waajemi na Waamedi kuchukua nchi. Danieli na wenzake wakasimama mbele ya mfalme, yaani, wakatumika katika ikulu ya Babeli.

*Kuna nafsi ambazo zimepoteza ujasiri wao; zungumza nao, uwaombee. Kuna wanaohitaji Mkate wa Uzima. Wasomee kutoka katika Neno la MUNGU. Kuna ugonjwa wa roho ambao hakuna zeri inayoweza kuugusa, hakuna dawa inayoweza kuponya. Waombee hawa, na uwalete kwa Yesu Kristo. Na katika kazi yako yote Kristo atakuwepo kufanya ushawishi kwenye mioyo ya wanadamu.


---

Kwa nini Danieli na wenzake walichukuliwa utumwani? Mfalme gani alitawala? Mkuu wa matowashi aliwaambia wafanye nini? Vijana hawa waliomba wapewe chakula gani? Kwa nini baadhi ya vyakula ni sumu kwa miili yetu?

**SIKU YA 161**
**(Juni 9)**

# Somo la Chakula

**- *Mwanzo 1:29 na Danieli 1***



Ufuatao ni muhtasari kwa ujumla kuhusu mambo ya chakula. Mzazi ndiye atakayeshughulikia zaidi ya mtoto. Ila inabidi tujue mambo haya na kuazimia kama Danieli.

Vijana wanne wanatuonesha mambo ya afya ambayo inabidi na sisi tujifunze. Waliweza kutawala nafsi zao na tamaa, bila kula cho chote. Dhambi ya kwanza bustani ya Edeni ilihusu chakula. Mtu anayeweza kutawala ulaji wake akiwa na uwezo wa kuwa na chakula anachotaka, ni shujaa. Asilimia kubwa ya magonjwa mengi inasemekana kutibika kwa chakula au lishe ya binadamu kwa namna moja au nyingine. Asilimia 80% ya mambo ambayo yanamwathiri mwanadamu afya yanahusiana na lishe kutokana na wataalamu wa Afya. Kwa nini ni muhimu kuwa na afya au kula chakula bora? Tukiwa na afya njema inatusaidia kuwa na akili bora ili tuelewe Neno la Mungu na masomo yetu darasani. Kuwa na afya kunapunguza gharama na pia kunasaidia kuhudumia wengine. Hatuwezi kusaidia jirani au ndugu kwa shughuli fulani kama tuko kitandani. Tukiwa na afya, inatufanya tuwe wacheshi na hata mahusiano yetu na watu yanapata faida. Pia inatusaidia tusiwe tegemezi kwa wengine, na mara zingine kutegemea wengine kutokana na ulema au uzee, hutokea, ila lisiwe jambo ambalo tumechangia litokee kwa neema ya Mungu! Na kuna wengi ambao hufa kwa uzee na si ugonjwa. Peleleza zaidi kuhusu hilo!

Asilimia 50-80% ya chakula chako kiwe kisichopikwa, yaani, mbogamboga na matunda, kimea na vingine walivyokula vijana wanne wa Babeli. Bustani ya Edeni haikuwa na masufuria, usiharibu chakula chako mara zote kwa kupika, vile vinavyoweza kuliwa bila kupikwa, viliwe hivyo hivyo. Vyakula vya mbegu walivyokula viliwasaidia, kwa siku 10 tu wakawa bora mara 10 zaidi ya vijana wa rika lao. Fanya chakula chako kuwa dawa, na dawa yako kuwa chakula. Usikoboe chakula chako, mfano ngano, mchele, mahindi, kula mkate wa ngano isiyokobolewa, mchele wa brown, na dona. Sukari na mafuta pia ni vyakula vilivyokobolewa, yaani, ni vitu vimetolewa kwenye mmea na sio mmea mzima. Ili kupata kijiko kikubwa cha mafuta ya mahindi, inabidi tukamue mahindi 14 yaliyokuwa kwenye magunzi.

Ilikuwa mpango wa Mungu ule mahindi 5 ushibe, ila ukila chips 5 hivi utakuwa kama umekula mahindi 84 hivi (Chips ni viazi vya kukaanga). Kula matunda angalau matano kwa siku, ni vyema uwe na bustani ili ulime matunda kama nyanya, kama miti ni vigumu kuota kwako. Bustani ni muhimu sana uwe nayo. Kuona vitu vinakua bustanini ni tiba kwenye mawazo yetu. Milo miwili kwa siku ndiyo bora, labda uwe unafanya kazi nzito za mikono kama za shambani, au jeshini. Usipende kuigiza vyakula wanavyokula watu fulani, au tunavyoona kwenye runinga, haya ni maisha bandia. Vyakula vinaweza kuwa ni sawa isipokuwa utayarishaji unatofautiana na tamaduni. Mfano, Wahindi watapika chapati na ngano, Mwafrika atapika ugali. Mzungu atapika mkate. Vyakula vya watu wengi si vizuri. Usiigize, wewe kula vile Mungu alivyoumba bila ya kuvifanyia mambo mengi mengi. Mfano, tukipewa unga wa ngano, watu kwetu watapika ugali, India watapika chapati, wazungu watapika mkate. Ugali hauna chumvi wala mafuta, hivyo chenye afya kupita vyote pale itakuwa ugali, kama haujakobolewa. Ni vyema kuangalia mtu asiwe mnene au mwembamba sana, jaribu kuuliza mtumishi wa afya akwambie kutokana na urefu wako unapaswa uwe na kilo ngapi. Miili yetu ina maelekezo kutoka kwa Mungu kama vile ambavyo mashine zina na vitabu vya mwongozo wa jinsi ya kuzitumia.

Jitahidi usile ovyo ovyo chakula cha hotelini, maana wanaweka vitu vingi ili kufurahisha ladha ila si vya afya. Tunakula milo kama 1000 kwa mwaka, ni vyema mzazi wako, ajifunze kupika vizuri, ni bora mjue kupika kwa afya. Wengi wamekufa duniani kwa sababu ya vyakula vibovu. Epuka vyakula vilivyokobolewa, vyenye chumvi nyingi, sukari nyingi na mafuta mengi. Kifungua kinywa ni mlo muhimu sana, jitahidi mlo huu usikupite. Kula ushibe vizuri na usile mpaka saa tano au sita zipite. Jitahidi kula chakula cha jioni mapema, acha tumbo lako wazi angalau saa 4 kabla ya kulala. Unapokula chenza usifyonze maji tu, utakuwa kama umekoboa chenza.

Kuna vitu vingine kamwe visiingie mdomoni mwako kabisa, navyo ni kama mafuta ya taa, sabuni na vingine! Si hivyo tu bali pia pombe, madawa ya kulevya, sigara, nyama najisi kama nguruwe, kamba, kaa, tai, punda, mbwa, kunguru, kumbikumbi, chura, mijusi na vinginevyo kama Mambo ya Walawi 11 inavyosema. Samaki wa kula ni wale wenye magamba na mapezi. Kuku wengi na mifugo siku hizi inalishwa vitu ambavyo ni kinyume cha maumbile yao na kuwa wakubwa kwa haraka, wanyama wa namna hii, jieupushe kuwala. Kule Minesota, rafiki yangu alienda akaona bata mzinga wanapigwa sindano za homoni za wanawake ili wawe na vifua au vidari vikubwa. Ilikuwa mtindo wa wengi kupenda vidari, kwa vile havina mafuta, hivyo vikawa na soko. Basi aliona wengi wamekufa kwa kupasuka vifua. Alipouliza aliambiwa sababu. Pia, epuka kula chumvi nyingi.

Jifunze kula mbogamboga kama matango, karoti, beet root, mbegu, ufuta, alizeti, karanga, korosho na nazi. Rangi tofauti za mimea zina lishe tofauti, badilisha rangi za chakula chako. Nunua vitabu vya lishe na ujifunze. Pika vyakula vyako na ndimu, kitunguu saumu, tangawizi, manjano, kitunguu maji, sage, oregano, giligilani na mbegu zake (coriander) na viungo vingine vya asili ambavyo vina afya, pia itasaidia upunguze kuweka chumvi au mafuta. Epuka kukaanga vyakula. Ikiwa yabidi utumie mafuta, basi chagua yale ya mimea. Epuka margarine maana ina

haidrojeni na huifanya kuwa kama plastiki kwenye mwili. Vyungu ndiyo vizuri kwa kupikia au sufuria za Stainless Steel, masufuria mengine yanafanya tule chuma. Usipende kula vitu vya kwenye makasha au vilivyosindikwa, na kama inabidi ule, soma kwanza vitu vilivyomo (ingredients). Epuka kahawa, soda za aina zote na vitu vinavyosisimua mwili. Usilete ndani ya nyumba kitu ambacho si cha afya. Chukua tahadhari kuhusiana na mambo ya kula na kunywa. Uwe makini na matangazo mengi ya biashara za vyakula.

Sukari guru ni bora kuliko ile sukari nyeupe. Epuka vyakula vya makopo. Tafuna vizuri chakula hata mara 32. Pishanisha mboga za majani na matunda kadri uwezavyo kwani vyema mboga mboga zisichanganywe na matunda. Mfano usile karoti pamoja na matunda, viyeyushio yaani enzymes zilizo tumboni zinazotumika, huwa tofauti, na hivyo unalichosha tumbo, Usile na kunywa maji hapohapo, pitia nusu saa au zaidi kabla ya kunywa maji. Usile bazooka au bubble-gum, inaleta gesi na kuharibu tumbo. Tunakula ili tuishi na hatuishi ili tule. Epuka vitu vya sukari kama peremende na keki, ziwe nadra sana. Usile nyama kibudu, yaani asiyechinjwa. Usile vikolezo vya achari, pilipili, haradali, siki. Mengineyo ya afya ni kufanya mazoezi, kunywa glasi 8 na zaidi za maji kwa siku, pata muda wa kupumzika, uwe mtu wa kiasi, jali usafi, pata mwanga wa jua na hewa safi, na kumtumaini Mungu. Maana hata ukifanya ya afya yote, Mungu hataokoa wenye dhambi wenye afya.

Tunapenda kusisitiza kwamba afya ya muhimu isiyoisha ni uzima wa milele. Tunashughulikia afya zetu ili mawazo yetu yawe safi na kuweza kulielewa Neno la Mungu. Mtu anayeweza kujitawala nafsi yake kwa chakula, anaweza kushinda majaribu mengi. Panga muda wa kuomba na kufunga, inakupa afya. Soma uelewe zaidi tiba rahisi, lakini utumie tiba rasmi pale inapobidi maana sote tunahitaji kupimwa na tabibu, kuchukua vipimo na kusaidiwa na tiba ya magharibi (conventional medicine) kwenye dharura, mfano kuvunjika mguu. Mengineyo angalia kwenye amazinghealth.com au NEWSTART.

*Oh, jamani kama sala ya dhati na ya imani ingetokezea kila mahali, Nipe roho zilizozikwa sasa kwenye uchafu wa makosa, la sivyo nife! Walete kwenye ujuzi wa Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu.


---

Kwa nini ni muhimu kula chakula bora? Dhambi iliingiaje Edeni? Afya ya muhimu ni ipi? Taja aina 10 za mboga mboga. Taja aina 15 za matunda. Taja aina 10 za nafaka. Taja aina 5 za jamii ya njugu? Taja aina 10 ya jamii za kunde. Vyakula vilivyokobolewa ni vipi? Kwa nini tuepuke peremende? Kwa nini kupika chakula kunapunguza nguvu zake? Kazi gani hazitakuwapo mbinguni?

**SIKU YA 162**
**(Juni 10)**

# Mfalme Aota Ndoto

**- Danieli 2**



Katika mwaka wa pili wa kumiliki kwake, Nebukadreza, mfalme wa Wakaldayo, aliota ndoto; na roho yake ikafadhaika, usingizi wake ukamtoka. Ndipo mfalme akatoa amri ya kuwaita waganga, wachawi, wasihiri na wanajimu wapate kumweleza ndoto yake. Mfalme huyu alikuwa hamjui Mungu wa mbinguni vizuri ndiyo maana akaleta hawa watu wanaotumia nguvu za giza ili kumfunulia ndoto yake. Walipoingia, mfalme aliwaambia kuwa ameota ndoto, naye amefadhaika sana na anataka ajue ile ndoto na tafsiri yake. Hawa Wakaldayo wakamwambia kwa lugha ya Kiaramu, "Ee Mfalme, uishi milele, tuambie sisi watumishi wako ile ndoto, nasi tutakuonyesha tafsiri yake." Pengine hata nawe umewahi kuota ndoto siku fulani, ukashindwa kukumbuka ndoto yako. Ndoto hii ilikuwa na maana nzito, kwani Mungu alikuwa amemfunulia mfalme mambo ya siku za usoni. Mungu alimtumia kwa njia nyingi, hata hatimaye aliongoka. Mfalme huyu aliambiwa na Mungu Mwenyewe awachukue Wayahudi mateka ili wapate adhabu kwa sababu ya uasi na kuabudu miungu mingine. Na sasa Mungu akamfunulia mfalme unabii ambao ni kati ya unabii mrefu kupita yote.

Kuanzia Nebukadreza alipotawala mpaka mwisho wa dunia. Hakika Mungu hana upendeleo. Mfalme akasema, ndiyo maana amewaita, kwa sababu ndoto yenyewe imemtoka, wasijidai wanapoteza wakati. Akawaambia "msiponijulisha ile ndoto na tafsiri yake, mtakatwa vipande vipande, na nyumba zenu zitafanywa jaa." Akasema kama wakimwonyesha ile ndoto na tafsiri yake, atawapa zawadi na thawabu na

heshima nyingi. Akawaonya tena, kwamba iko amri moja tu iwapasayo, maana wamepatana kusema maneno ya uongo na maneno maovu mbele yake hata zamani zitakapobadilika, akawahimiza wamwambie ndoto haraka. Wale watu wakamjibu kwamba hakuna mtu duniani awezaye kuonesha ndoto ya mtu aliyoota, iwe mchawi, mganga au Mkaldayo, ila miungu wasioishi na binadamu. Basi mfalme akapata hasira, na akatoa amri kuwaangamiza wenye hekima wote wa Babeli, na amri ikatangazwa kwamba saa ya kuuwawa ni karibu. Wakamtafuta Danieli na wenzake ili wauawe. Alitafutwa kwa sababu hakuwepo wakati huu mambo yakiendelea.

Danieli kwa busara akamjibu Arioko, akida wa walinzi wa mfalme, aliyekuwa amekuja kutimiza amri ya kuwaua wenye hekima wa Babeli. "Mbona amri hii ya mfalme ina ukali namna hii." Arioko akamwarifu Danieli habari ile. Ndipo Danieli akaenda kumwona mfalme na kuomba apewe muda, kisha yeye atamwonyesha mfalme ile ndoto na tafsiri yake. Danieli akaenda kwake, na kuwapasha wenzake Hanania, Mishaeli na Azaria, ili waombe rehema za Mungu wa mbinguni kwa habari ya siri ya ndoto ile, ili wasiangamizwe pamoja na wenye hekima wa Babeli. Ndipo Danieli alipofunuliwa siri hiyo katika njozi ya usiku. Danieli akamhimidi Mungu wa mbinguni akisema, "Na lihimidiwe Jina la Mungu milele na milele, kwa kuwa hekima na uwezo ni wake. Yeye hubadili majira na nyakati; huuzulu wafalme na kuwamilikisha wafalme, huwapa hekima wenye hekima; huwapa wenye ufahamu maarifa; Yeye hufunua mambo ya fumbo na ya siri; huyajua yaliyo gizani, na nuru hukaa Kwake. Nakushukuru, nakuhimidi, Ee Mungu wa baba zangu, uliyenipa hekima na uwezo, ukanijulisha hayo tuliyotaka Kwako; maana umetujulisha Neno lile la mfalme." Danieli akamshukuru Mungu, kisha akaenda kwa Arioko aliyeagizwa kuwaua wenye hekima wa Babeli kama ndoto isipopata ufumbuzi. Akamwambia, "Usiwaangamize wenye hekima wa Babeli, niingize mimi mbele ya mfalme, nami nitamwonyesha mfalme ile tafsiri." Arioko akashusha pumzi moyoni na kushukuru, akamwingiza Danieli kwa mfalme haraka. Akamwambia mfalme, "nimemwona mtu wa hao wana wa Yuda waliohamishwa atakayemjulisha mfalme ile tafsiri."

Mfalme akamwuliza Danieli, "Je! waweza kunijulisha ile ndoto niliyoona na tafsiri yake?" Danieli alijibu kwa unyenyekevu, "wenye hekima hawawezi kumfunulia mfalme, wala wachawi, wala waganga, wala wanajimu; lakini Yuko Mungu mbinguni afunuaye siri, Naye amemjulisha mfalme Nebukadreza mambo yatakayokuwa siku za mwisho." Somo tunalojifunza hapa ni kutojikuza, kwamba sisi tunaweza, bali tumpe Mungu utukufu.

Siku hizi wengi wasema wanatabiri ya mbele, kwa kusoma nyota au mikono; usiende kwa wabashiri wa namna hii. Piga magoti umwombe Mungu ili akufunulie mambo yaliyofichika. Maisha ya Danieli yalikuwa ya maombi.

Sala ya Danieli ilikuwa ni yenye Ufanisi, unyofu na Nguvu—Danieli alimwomba MUNGU, na hakujiinua mwenyewe au kudai wema wowote: "Ee Bwana, sikia; Ee Bwana, samehe; Ee Bwana, sikiliza na utende; usichelewe, kwa mapenzi Yako, Ee MUNGU wangu. " Maombi yake yalikuwa ya dhati na bidii. Katika kujibu ombi lake, Danieli alipokea nuru na Ukweli ambao yeye na watu wake walihitaji zaidi,

na pia mtazamo wa matukio makuu ya wakati ujao, hata ule ujio wa Mkombozi wa ulimwengu. Watu wote wanaompenda Mungu wanapaswa kuwa na hamu ya kuchunguza Maandiko au kupigana mieleka na Mungu katika maombi ili kupata uelewa wa wazi wa ile Kweli ya Biblia, na kutakaswa nayo.

* Anzeni kuombea roho; njooni karibu na Kristo, karibu na ubavu Wake unaotoka damu. Hebu roho ya upole na utulivu iyapambe maisha yenu, Hebu maombi yenu ya dhati na bidii, yaliyopondeka, ya unyenyekevu yapande Kwake kwa ajili ya hekima ili mpate kufanikiwa katika kuokoa sio nafsi zenu tu, bali na nafsi za wengine.

---

Danieli, Anania, Mishaeli na Azaria walitoka wapi? Mfalme alisema nini kitatokea kwa wenye hekima? Kwa nini Arioko alifurahi? Ni nani pekee awezaye kufunua mambo ya siri?

**SIKU YA 163**
**(Juni 11)**

# Falme Zitakazotawala Dunia

**- Danieli 2**



Danieli akasema, Ndoto yako, na njozi za kichwa chako ulizoziona kitandani pako, ni hizi; Wewe, Ee mfalme, mawazo yako yaliingia moyoni mwako kitandani pako ya mambo yatakayokuwa siku za baadaye, na Yeye afunuaye siri, Mungu, amekujulisha yatakayokuwa. Danieli akasema yeye hakufunuliwa siri hii kwa sababu ya hekima aliyo nayo kuliko wengine, bali kusudi mfalme afunuliwe ile tafsiri ya ndoto aliyoiota. Akamwambia mfalme kuwa, aliona na tazama kulikuwa na sanamu kubwa sana, na mwangaza wake mwingi, ikisimama mbele yake. Na umbo lake lilikuwa la kutisha, na sanamu hiyo kichwa chake kilikuwa cha dhahabu safi, na kifua chake na mikono yake ni fedha, na tumbo na viuno vyake ni shaba, na miguu yake ni ya chuma na nyayo za miguu yake ni nusu chuma, nusu udongo. Na tazama jiwe likachongwa bila kazi ya mikono ya mwanadamu, na jiwe hilo likaipiga sanamu miguu yake, iliyokuwa ya chuma na udongo, na kuivunja vipande vipande. Ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba, na ile fedha, na ile dhahabu, vilivunjwa vipande vipande na kuwa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari. Upepo ukavipeperusha hata pasionekane mahali pake. Na lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu likawa mlima mkubwa, likaijaza dunia yote. Danieli akamaliza kuelezea ile ndoto akisema, “hii ndiyo ile ndoto, nasi tutaihubiri tafsiri yake mbele ya mfalme.” Ikawa kama mfalme anaangalia tukio kwenye runinga pale alipokaa akielezwa mambo haya ya siku zijazo mpaka mwisho wa wakati.

Akasema, tafsiri ni kwamba yeye, mfalme Nebukadreza, ndiye mfalme wa wafalme wa dunia, maana alikuwa anatawala dunia nzima iliyojulikana wakati ule. Akamwambia, ni Mungu, Ndiye aliyempa ufalme, uwezo, nguvu na utukufu. Na kila mahali wakaapo wanadamu, wanyama wa kondeni, na ndege, amewatia mikononi mwake, naye amempa miliki juu ya hao wote, yeye ni kichwa kile cha dhahabu. Na baada yake utainuka ufalme mwingine mdogo kuliko yeye, uliofananishwa na fedha. Kisha ufalme mwingine wa tatu wa shaba, utakaoitawala dunia yote. Na ufalme wa nne utakaokuwa na nguvu kama chuma, kwa maana chuma huvunja vitu vyote na kuvishinda. Na kama alivyoona nyayo za miguu, na vidole vyake, kuwa nusu udongo wa mfinyazi na nusu chuma, ufalme ule wa chuma utakuwa umegawanyika, lakini ndani yake kutakuwa na nguvu za chuma, lakini kitakuwa kimechanganyika na udongo. Ikiwa na maana ufalme ule utakuwa na nguvu za chuma na nusu utakuwa umevunjika. Na kama vile alivyoona kile chuma kimechanganyika na udongo, vile vile watu watajichanganya nafsi zao kwa mbegu za wanadamu, lakini hawatashikamana kama vile chuma na udongo visivyoweza kushikamana.

Na katika siku za wafalme hawa wa mwisho wa chuma na udongo, Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme Wake, ikiwa na maana kwamba chuma na udongo ndiyo ufalme wa mwisho kabla ya mwisho wa dunia. Ufalme wa Mungu ndio ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake, bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele. Basi Mungu aliye mkuu amemjulisha mfalme mambo yatakayokuwa baadaye, mpaka siku za mwisho wa dunia. Ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti.

Ndipo mfalme Nebukadreza, akamsujudia Danieli, akijua Mungu yu pamoja naye, akatoa amri wamtolee Danieli sadaka na uvumba. Mfalme akasema, "Hakika Mungu wenu Ndiye Mungu wa miungu, na Bwana wa wafalme, awezaye kufumbua siri, kwa kuwa wewe uliweza kuifumbua siri hii. Basi mfalme akamtukuza Danieli, akampa zawadi kubwa nyingi sana, akamfanya kuwa mkubwa juu ya uliwali wote wa Babeli, na mkuu wa wenye hekima wa Babeli. Danieli akamwomba mfalme awaweke rafiki zake Anania, Mishaeli na Azaria wawe juu ya mambo yote ya uliwali Babeli, lakini Danieli yeye aliketi katika lango la mfalme. Danieli hakumsahau Mungu na hata marafiki zake. Je, unapenda kuwa bora mara kumi kuliko rika lako? Je, unapenda kujua yale yatakayotokea siku hizi za mwisho? Soma Neno Lake na ulifuate, utakuwa bora mara kumi na kujua siri za mbinguni.

*Nafsi zinapaswa kutafutwa, kuombewa, kufanyiwa kazi. Rufaa za dhati zinapaswa kufanywa. Maombi ya dhati yanapaswa kutolewa. Maombi yetu dhaifu, yasiyo na roho yanapaswa kubadilishwa kuwa maombi ya dhati n a bidii sana.

---

Kwa nini Danieli hakujisifu kwamba yeye ndiye anaweza mambo ya kutafsiri ndoto? Elezea ndoto ya mfalme? Tafsiri yake ni nini? Rafiki za Danieli walipata kazi gani? Kwa nini unafikiri wenye hekima wa Babeli walimshukuru Danieli?

**SIKU YA 164**
**(Juni 12)**

# Umuhimu wa Unabii wa Danieli 2

Vitabu vyote vya historia ya dunia vinatuambia kuwa Babeli ilitawala dunia, yaani kile kichwa cha dhahabu, kuanzia mwaka 606 KK-539 KK. Kisha Belshaza alitawala Babeli, kisha wakaja Wamedi na Waajemi. Walikuja na kuwapindua Wakaldayo na kuchukua nchi, chini ya Dario, waliingia mjini kupitia mto Frati, wakakuta karamu inaendelea na watu wamelewa, wala hawana habari. Walipotawala Waajemi, mfalme Koreshi alitoa mbiu ya wana wa Yuda kurudi katika nchi ya ahadi, na Zerubabeli, Yoshua, Nehemia, na Ezra wakawa miongoni mwa wale waliorudi, japo walirudi kwa nyakati tofauti. Utawala wa Wamedi na Waajemi ulianza mwaka 539KK-331KK. Inaonekana Danieli na wenzake waliridhika kukaa kule, kwani walikuwa hawatajwi popote kuwa miongoni mwa waliorejea. Baada ya ufalme huo wa Wamedi na Waajemi, ulifuata ufalme wa Wagiriki au Wayunani chini ya Alexander mkuu wa Makedonia, ambaye aliteka nchi nyingi. Alexander alikufa akiwa kijana wa miaka 32, kwa sababu ya ulevi. Alikuwa ameweza kuteka nchi nyingi, lakini alishindwa kutawala nafsi yake kwa ulevi. Baada yake, ufalme wake uligawanyika chini ya majemadari wake wa vita wanne waitwao Lysimachus, Cassander, Ptolemy na Seleucus. Waliigawa nchi vipande vinne, kila mmoja akatawala kimoja. Wayunani walitawala mwaka wa 331KK-168 KK. Baada ya Uyunani, ulifuata ufalme wa Warumi ambao walitawala dunia nzima inayojulikana, mwaka 168 KK-476 KK. Hata Kristo alizaliwa wakati Rumi inatawala chini ya Kaisari Agusto ambaye aliamuru watu wakaandikishwe katika miji yao. Maria na Yusufu walienda Bethlehemu ya Yuda na hivyo Yesu alizaliwa hapo. Ufalme huu wa Rumi ulibadilisha mambo mengi kama vile, siku kuanza saa sita ya usiku badala ya jioni kama ilivyo katika Biblia, na pia kubadilisha siku ya mapumziko kwenda siku ya kwanza ya juma.

Baada ya hapo ufalme wa Rumi uligawanyika katika falme kumi, kama vile vidole kumi vya miguu, lakini hazikuwa na nguvu sana kama vile chuma kilivyokuwa peke yake. Falme hizi kumi zilikuwa za Ulaya nazo ni kama Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Utaliano, Ureno, Uhispania, na Uswisi, na tatu ambazo leo hazipo (Vandal, Heruli na Ostrogoths).

Wafalme wa nchi hizi kama vile Charlmagne, Napoleoni na Hitler, walijaribu kuzifanya ziungane lakini hawakuweza. Kuna wakati Malkia wa Uingereza alijulikana kama mama wa wote Ulaya, kwani alikuwa na ujamaa na kila ufalme wa Ulaya. Walijaribu kuoza watoto wa kifalme wa nchi hizi kama Uingereza, Ujerumani, na Hispania, lakini hazikuweza kuwa pamoja. Hata vita kuu mbili za dunia vilitokea kwa nchi hizi kuanza kugombana na mataifa mengine yakajikuta yameingia. Vita kuu ya pili iliua zaidi ya watu milioni 50.

Hata leo wameanzisha muungano unaoitwa Umoja wa Ulaya, na shida ni ileile

"kama vile unavyoona chuma kisivyoweza kushikamana na udongo …." Nchi hizi zimetawala dunia kwa miaka mingi, hata Waingereza walijivuna wakisema, "Jua la Mwingereza halitui, kwani walikuwa na makoloni dunia nzima. Acheni Mungu aitwe Mungu, alitabiri na kimekuwa. Mungu anatabiri na inatokea…Hivi karibuni Uingereza imejitoa kwenye jumuiya ya Ulaya!

Unabii wa Danieli 2 unamalizia kwa kusema, "Na katika siku za wafalme hao Mungu atausimamisha ufalme Wake ambao hautaangamizwa milele." Tumefikia wakati huo, na Yesu alisema tuangalie dalili. Falme zote zimetawala, iliyobaki ni Mungu kusimamisha ufalme Wake. Dalili kwamba Mungu Yu karibu kufanya vile ili tuishi Naye milele na milele mbinguni ni nyingi. Injili kuhubiriwa ulimwenguni, maasi kuongezeka, matetemeko; wataalamu wa matetemeko wa Uingereza wanasema kuwa matetemeko yalikuwa 15 tu karne ya kwanza mpaka karne ya kumi na tano, na 378 kwa karne ya kumi na saba tu, ila karne hii ambayo tumemaliza, imekuwa na matetemeko 2119. Kutakuwa na vita na tetesi za vita, ufalme utatoka kupigana na ufalme, na haya yote tunayaona. Kitabu cha Timotheo kinaonesha kwamba siku za mwisho zitakuwa za hatari. Maana watu watakuwa "wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukurani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiaziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu Zake, wajifunzao ila wasiweze kufikia ujuzi wa Kweli, wanaopingana na kweli na kuharibikiwa na akili zao."

Kama vile zilivyokuwa siku za Nuhu ndiyo itakavyokuwa siku zetu, watu walikuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa. Kama ilivyokuwa kwa Sodoma, haya tunayasikia na kuyaona kwenye vyombo vya habari (kama redio, magazeti, kompyuta) na hata kwenye vitabu. Watu wakiishi bila ndoa, na kuingia katika ngono chafu. Zote hizi ni dalili za dunia kwisha. Kila kukicha kuna mambo mengi ya kutisha, mafuriko, au magonjwa kama Ebola. Usalama wetu ni kumtumaini Mungu tu aliye amani yetu na uzima wa milele.

Tuna dalili moja nzuri ya ufalme wa Mungu kukaribia, nayo ni habari njema kuhubiriwa kila mahali. Biblia imetafsiriwa kwa lugha nyingi, na watu wanaendelea kuwaambia wengine habari njema za ufalme. Teknolojia na mtu kwa mtu vinatumika. Hata wewe leo Mungu anakutaka uwaeleze watu habari njema za ufalme.
Ndoto aliyoiona Nebukadreza, haikumhusu yeye tu na wale watu wa Yuda, bali ilituhusu sisi pia. Ilieleza mwisho wa yale mapambano kati ya Shetani na Mungu au wema na uovu. Ujumbe huu ni wa kutia moyo kwamba baada ya mataifa kutawala, Mungu atausimamisha ufalme Wake wa upendo, amani, furaha na utulivu ambao utadumu milele. Je! umeanza kujitayarisha ili uwe katika ufalme huo?

*azi hii inakuhitaji uzilinde roho kama yule ambaye lazima utazitolea hesabu. Upole wa Kristo lazima uujaze moyo wa Mfanyakazi wa Sala ya Maombezi. Ikiwa una upendo kwa roho utaonyesha kujali kwa dhati kwa ajili yao. Utatoa maombi ya unyenyekevu, ya dhati, ya kutoka moyoni kwa wale unaowatembelea. Harufu ya upendo wa Kristo itadhihirishwa katika kazi yako. Yeye ambaye alitoa maisha Yake



kwa ajili ya maisha ya ulimwengu atashirikiana na mtenda kazi asiye na uchoyo au ubinafsi kuweka msukumo juu ya mioyo ya wanadamu.

---

Kichwa cha dhahabu kinasimamia nini? Kifua na mikono ya fedha inasimamia nini? Tumbo na mapaja ya shaba yanasimamia nini? Miguu ya chuma inasimamia nini? Vidole vya udongo na chuma vinasimamia nini? Leo sisi tuko wapi kwenye sanamu hii? Tunapata fundisho gani kuhusu unabii huu?

**SIKU YA 165**
**(Juni 13)**

# Kurudia unabii wa Danieli 2 kwa undani zaidi

Unabii wa kustajaabisha wa nchi zote zitakazotawala ulimwengu kabla ya Mwisho wa dunia.
Sanamu aliyoiota mfalme na tafsiri yake (soma Daniel 2)
Kwaajili wakati tunaoishi sasa hivi ni ukingoni kabisa ukisoma huu unabii, tungependa tena turudie unabii huu kwa ndani zaidi. Nawe pia uchukue muda kuusoma, kwani hauna mafumbo mengi. Mambo mengi yako wazi. Na tawala hizi ni zile ambazo unaweza ukarejea kwenye vitabu vya historia na kuona mambo yalivyo halisi.
MCHORO wa sanamu ya ndoto ya Nebukadneza

YOTE yanayotabiriwa na MUNGU hutokea

Unabii wa Kale Wadhihirisha Wakati Ujao

Mojawapo miongoni mwa unabii wa kale kabisa ulimwenguni huelezea kuwa sayari yetu inakaribia kushuhudia tukio kubwa la kustaajabisha katika historia ya mwanadamu: mwisho wa falme kama tunavyoufahamu unabii huo. Unabii huu hautaji tarehe maalumu—wala mwaka wala muongo wala hata karne. Hata hivyo, maelezo yake ya historia ya mwanadamu yamekuwa sahihi sana kiasi kwamba hatua ya mwisho—moja pekee iliyobakia kutimia—ni hakika kabisa.

Kisa huanza kwa tukio la kusikitisha la uhamisho wa maelfu ya Wayahudi kutoka nchi yao huko Palestina.* Miongoni mwa mateka ambao Mfalme Nebukadneza aliwachukua kwenda Babeli walikuwa vijana wadogo wanne wa kifalme: Danieli, Shadraka, Meshaki, na Abednego. Katika hali inayoonekana kuwa ya ajabu kwetu, lakini iliyokuwa ya kawaida katika kipindi hicho, Nebukadneza aliwaandikisha vijana hawa wanne katika "Chuo Kikuu cha Babeli" ili wapewe mafunzo ya kuwa washauri wa mfalme.

**Ndoto ya Nebukadneza**
Muda mfupi baada ya haya, mfalme aliota ndoto. Kwa kweli, ilikuwa ndoto ya kuogofya iliyomsumbua sana, lakini hakuweza kuikumbuka alipoamka asubuhi iliyofuata. Akiwa ameshawishika kuwa ndoto ile ilikuwa muhimu sana, Nebukadneza aliwaita washauri wake na kuwaamuru wamwambie kuhusu kile alichokuwa ameota na maana ya ndoto yake.

"Wenye hekima" hawa wakapinga agizo hili la kustaajabisha. Lakini mfalme akasema, "Ama mniambie ndoto hiyo, la sivyo nitaamuru mwuawe!" Licha ya tishio la kifo, hata hivyo, washauri wa mfalme hawakuweza kupata jibu nzuri.
Wakati huo, Danieli na marafiki zake watatu walikuwa hawakuitwa ikulu ya mfalme pamoja na wale washauri wa mfalme. Hata hivyo, huenda kwa sababu walikuwa

ni wenye-hekima-mafunzoni, amri hii iliwahusisha wao. Wakati askari walipokuja kuwakamata, Danieli aliomba apewe muda zaidi. Ombi lake lilikubaliwa, na usiku uleule Mungu alimuonesha Danieli ndoto ile aliyoiota Nebukadneza. (Mungu ndiye aliyekuwa amempatia Mfalme ndoto hiyo). Asubuhi iliyofuata askari akamleta Danieli kwa mfalme.

### Danieli aifafanua ndoto

Baada ya taratibu za salamu kumalizika, Danieli akamwambia mfalme ile ndoto aliyokuwa ameiota: "Wewe, Ee Mfalme, uliona, na tazama, sanamu kubwa sana…. Na sanamu hii kichwa chake kilikuwa ni cha dhahabu safi; kifua chake na mikono yake ni ya fedha; tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba; miguu yake ni ya chuma; na nyayo za miguu yake nusu ya chuma na nusu ya udongo. Nawe ukatazama hata jiwe likachongwa bila kazi ya mikono, nalo jiwe hilo likaipiga sanamu miguu yake, iliyokuwa ya chuma na udongo, likaivunja vipande vipande. Ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba, na ile fedha, na ile dhahabu, vilivunjwa vipande vipande pamoja vikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari; upepo ukavipeperusha hata pasionekane mahali pake; na lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu likawa milima mikubwa, likaijaza dunia yote" (Danieli 2:31-35).

Kimsingi, mfalme alikuwa na shauku ya kujua maana ya ile ndoto. Maelezo ya mwanzo ya Danieli lazima yalikuwa yamemjaza kiburi: "Wewe, Ee mfalme,… u kichwa kile cha dhahabu." Lakini maneno yake yanayofuata hayakuwa ya kutia moyo kiasi hicho: "Na baada ya zamani zako utainuka ufalme mwingine mdogo kuliko wewe." Danieli alielezea hayo yote, falme tatu zingefuata baada ya Babeli. Watafsiri wengi wa Biblia wanakubali kuwa falme hizo huwakilisha Uamedi-Uajemi, Uyunani, na Rumi.

Lakini Rumi ilikuwa ya mwisho katika mfululizo wa falme zenye nguvu. Ilipoanguka, masalia yake yakawa mataifa mbalimbali ya Ulaya, Afrika Kaskazini, Mashariki ya Kati ambayo tunayafahamu hadi hivi leo. Uangamivu uliosababishwa na lile jiwe kwenye sanamu huwakilisha uangamivu wa mataifa haya mwisho wa dunia, ambapo baadaye Mungu atausimamisha Ufalme Wake Mwenyewe wa milele.

### Nini Kinachoshangaza Sana?

Hapa kuna jambo linalostaajabisha sana kuhusu unabii huu. Danieli aliandika unabii huu takriban mwaka wa 600 KK. Alikuwa anauelewa kuhusu Babeli kwa kuwa aliishi huko, na huenda aliifahamu Uamedi na Uajemi katika kipindi alichoandika unabii huu—ingawa utawala huo haukuiangusha Babeli mpaka miaka kadhaa baadaye. Lakini kibinadamu, hakuna namna yoyote ambayo Danieli angeliweza kutabiri kuinuka na kuanguka kwa Uyunani na Rumi au kuvunjika kwa himaya ya Kirumi. Lakini kila kitabu cha sekondari cha historia ya ulimwengu hushuhudia kuwa ndoto ya Nebukadneza ilitimizwa vilevile hasa kama Danieli alivyomfunulia Mfalme!

Baadhi ya wafafanuzi wa Biblia hudai kuwa Danieli aliiandika ndoto yake takribani miaka mia moja na hamsini tu kabla ya Kristo, badala ya miaka 600 KK., kama anavyodai. Hivyo, wanasema, hakuna lolote la kimwujiza kuhusu maelezo yake ya

kihistoria. Lakini hata kama Danieli alikuwa ameandika unabii wake mwaka 650 KK., hakuna namna yoyote ambayo ingemsaidia kufahamu kuhusu kuvunjika kwa himaya ya Kirumi na kuwa mataifa mbalimbali, tukio lililofanyika miaka mia nne baadaye.

Hivyo, ukweli wa kushangaza unatukabili: Nabii aliyeishi zaidi ya miaka elfu mbili na mia tano iliyopita aliangalia mbele katika kipindi cha miaka mingi baadaye na kutupatia maelezo sahihi kabisa ya matukio ya siku zijazo.

Hatuwezi kufanya hitimisho lingine lolote kutokana na hoja hii zaidi ya kusema kuwa Danieli aliyapokea maelezo haya ya matukio ya siku zijazo kutoka kwa Mungu Mwenyewe. Na kwa sababu kila kitu katika maelezo ya Danieli juu ya historia ya ulimwengu kimetimizwa, tunaweza kuwa na hakika kuwa tukio la mwisho—mwisho wa dunia kama tunavyoufahamu na kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu Mwenyewe—litatokea pia. Hivyo ni vyema tujitayarishe na ujio wa ufalme wa MUNGU utakaodumu milele zote, kwani maisha ya sasa ni ya muda mfupi tu!
*Danieli sura ya 2 huelezea unabii huu. Danieli sura ya 1 huelezea utangulizi wa matukio haya. ( Kwa masomo zaidi andika kwa Kibidula Mission, P.O Box 17, Mafinga, Tanzania).

*Waombee Wengine Katika Ombi la faragha—Katika ombi la faragha wote wana fursa ya kuomba kadri wapendavyo na kuwa wazi wapendavyo. Wanaweza kuomba kwa ajili ya jamaa na marafiki zao wote. Chumbani ni mahali pa kueleza shida zao zote binafsi, na mitihani, na majaribu. Mkutano wa pamoja wa kumwabudu MUNGU si mahali pa kufungua mambo binafsi au siri za moyoni.

---

Kwanini ni muhimu kuusoma Unabii wa Danieli 2? Ni jambo gani linatuonyesha kwamba unabii huu uko njiani kutimia siku za karibuni? Je! Wewe leo unapanga kujitayarishaje na ujio wa YESU?

**SIKU YA 166**
**(Juni 14)**

# Kulazimishwa Kusujudu Sanamu

**- Danieli 3**

Baada ya kupewa tafsiri nzuri na ya ajabu, na hata mfalme akaanza kumtukuza Mungu wa mbinguni, mfalme alipata jaribu la kiburi. Bila shaka aliwaza ile sanamu usiku na mchana, akitaka ufalme wake uwe wa milele. Akaona miaka hiyo sabini au ya kichwa tu haimtoshi, akataka atawale milele na watu wamsujudie. Akapata wazo la kutengeneza mfano wa ile sanamu aliyoiona, ila badala ya kuweka madini tofauti, yeye aliifanya ya dhahabu tupu kuanzia miguu mpaka kichwani. Akimaanisha kuwa utawala Wake utakuwa wa milele! Ila hakuna binadamu anaishi milele, au nchi inayotawala milele, ni ufalme wa Mungu peke yake utakuwa wa milele.

Mfalme akatoa amri kwamba sanamu hii ya urefu wa dhiraa sitini na upana wake dhiraa sita isimamishwe katika uwanda wa dura na viongozi wote waje ili kuizindua. Bila shaka watu walijiuliza kuwa mfalme atafanya nini na sanamu hii. Mara ilipokamilika, mfalme alitangaza kuiizindua ile sanamu, na manaibu, maliwali, maamiri, watunza hazina na wengine walikusanyika pale. Mpiga mbiu akawaambia, "Enyi watu wote mmeamriwa hivi … mtakaposikia sauti ya panda, filimbi, kinubi, zeze, santuri, zomari, ngoma, lazima kuanguka na kuiabudu sanamu ya dhahabu, mfalme Nebukadreza aliyoisimamisha. Na kila mtu asiyeanguka na kuabudu atatupwa saa hiyo hiyo katika tanuru la moto uwakao." Basi watu wa kabila zote waliposikia sauti za vyombo hivyo, wakaanguka wakaiabudu ile sanamu, mfalme Nebukadreza aliyoisimamisha."

Baadhi ya Wakaldayo walileta mashitaka kwa mfalme wakisema, "Ee mfalme uishi milele, ulitoa amri ya kwamba kila mtu atakapoisikia sauti ya panda, na filimbi, na kinubi, na zeze, na santuri, na zomari, na namna zote za ngoma, ni lazima aanguke na kuiabudu ile sanamu ya dhahabu; na kila mtu asiyeanguka na kuabudu atatupwa katika tanuru ya moto uwakao."

Wakasema kuna Wayahudi kadha wa kadha aliowakweka juu ya majimbo ya wilaya za Babeli nao ni Shadraka, Meshaki na Abednego, hawajali wala kutumikia miungu yake mfalme. Inawezekana watu walianza kuwaangalia hao Wayahudi waliokaidi amri ya mfalme. Nebukadreza akatoa amri kwa hasira waletwe kwake. Walipoletwa akasema, "Enyi Shadraka, na Meshaki na Abednego, je! Ni kwa makusudi hata hammtumikii mungu wangu wala kuijudia sanamu ya dhahabu niliyosimamisha?" Vijana hawa hawakutaka kuvunja amri ya pili. Mfalme akawapa nafasi tena kwamba wakisikia sauti za vyombo vya muziki safari hii waanguke na kuisujudia sanamu yake. Mfalme alijisahau sana, baada ya matendo makuu ya Mungu wa mbinguni, sasa anarudi kujiabudu mwenyewe. Akarudia tena kuwa wasipoanguka na kuisujudu ile sanamu, basi watatupwa saa iyohiyo katika tanuru



iwakayo moto, akasema, “naye ni nani Mungu yule atakayewaokoa ninyi na mikono yangu?” Ndipo Shadraka, na Meshaki na Abednego wakamwambia mfalme, kwamba hawahitaji muda wa kufikiri zaidi katika neno hili, kwani walikuwa wameshaazimia la kufanya, kwamba hawataisujudia ile sanamu. Wakamwambia mfalme, “Mungu wetu tunayemtumikia aweza kutuokoa na tanuru ile iwakayo moto; Naye atatuokoa na mkono wako, Ee mfalme. Bali kama si hivyo, ujue, Ee mfalme, ya kuwa sisi hatukubali kuitumikia miungu yako, wala kuisujudia hiyo sanamu ya dhahabu uliyoisimamisha.”

Mfalme akajaa ghadhabu na uso wake ukabadilika juu ya hawa vijana watatu wa Yuda, na akaamuru watupwe kwenye moto na tanuru likokwe mara saba zaidi ya kawaida. Mfalme kwa amri kali aliwaambia mashujaa wa jeshi lake wawafunge hawa vijana watatu na kuwatupa katika ile tanuru iliyokuwa ikiwaka moto. Vijana hawa walifungwa wakiwa wamevaa suruali, kanzu na joho zao. Wakatupwa kwenye tanuru iliyokuwa na moto mkali, na mwako ule ukawaua wale mashujaa wa jeshi waliowatupa motoni. Shadraka, Meshaki na Abednego wakaanguka katikati ya tanuru ile inayowaka moto. Ndipo Nebukadreza akastajabu na kuinuka kwa haraka akisema, “Je! hatukutupa watu watatu, hali wamefungwa katikati ya moto?” Wakamjibu “Kweli Ee mfalme.” Mfalme akasema, “Tazama mimi naona watu wanne, nao wamefunguliwa, wanatembea katikati ya moto hali hawana dhara, na sura yake yule wa nne ni mfano wa mwana wa miungu.” Basi akasogea karibu na mdomo wa moto, akanena akasema, “Enyi Shadraka, na Meshaki, na Abednego, watumishi wa Mungu aliye juu, tokeni mje huku.” Je, wewe ungekuwa na Yesu ungependa kutoka motoni kweli? Basi wale vijana wakatoka, na watu wote wakaona kwamba ule moto ulikuwa hauna nguvu kwao, hata nywele zao hazikuteketea, wala nguo zao kubadilika au kuwa na harufu ya moshi hata kidogo. Kisa hiki watu walisimuliana tena na tena, na ingekuwa siku za redio na televisheni, kingekuwa kwenye habari! Vijana hawa walikuwa wamefuzu mtihani mwingine wa imani, wakiwa na miaka kumi na saba hivi walishinda mtihani wa afya, kwa kula vyakula bora. Ilikuwa imepita miaka zaidi ya 20 na pengine walikuwa na miaka 40 hivi.

Mfalme akasema, “Na ahimidiwe Mungu wa Shadraka, na Meshaki na Abednego; aliyemtuma malaika Wake, akawaokoa wale waliomtumaini, wakaligeuza neno la mfalme, na kujitoa miili yao ili wasimtumikie mungu mwingine, wala kumwabudu, ila Mungu wao wenyewe.” Mfame akaweka amri kwamba kila mtu wa kabila na lugha atakayenena neno lolote lisilopasa juu ya Mungu wa vijana hawa, atakatwa vipande vipande na nyumba yake itafanywa jaa. Kwa kuwa hakuna Mungu mwingine awezaye kuokoa namna hii. Kisha mfalme akawaongeza cheo Shadraka, na Meshaki na Abednego katika wilaya ya Babeli. Ushahidi wa ajabu kwa dunia nzima huyu mfalme aliyoitawala. Mungu hakuchelewa kuwaokoa watoto Wake. Kamba ziliungua lakini vinyweleo havikuungua. Acheni Mungu aitwe Mungu. Hebu na tumsujudu, kumwamini na kumtii. Kisa hiki kilileta matumaini kwa vijana mateka. Nawe hivi leo, Mungu anaweza kukufanyia makuu, dumu tu ukimtumaini.

*Wakati vijana wanapoenda kuhubiri Ukweli, mnapaswa kuwa na majira ya maombi kwa ajili yao. Omba kwamba MUNGU awaunganishe na Yeye Mwenyewe na awape

hekima, neema, na maarifa. Ombeni ili waweze kulindwa na mitego ya Shetani iliyojificha na kuwekwa safi katika mawazo na utakatifu wa moyo. Ninawasihi ninyi mnaomcha Bwana, msipoteze wakati katika mazungumzo yasiyofaa, au katika kazi isiyo na maana, ili kujipatia kiburi, au kuridhisha tamaa ya chakula au ya mwili. Hebu wakati unaopatikana utumike katika kupambana mieleka na MUNGU kwa ajili ya wachungaji/wahudumu wenu. Inueni mikono yao kama Haruni na Huri walivyoifanya mikono ya Musa.

---

Ni kosa gani mfalme Nebukadreza alilifanya? Kwa nini dhambi ya kiburi ni vigumu kuiona na kuiacha? Kwa nini wale vijana watatu walikataa kuabudu sanamu? Zawadi yao ya utii ilikuwa nini? Kwa nini hata sisi leo ni bora tuwe tayari kumtii Mungu hata kufa? Mfalme wa dunia alijuaje kuwa yule wa nne ni kama mwana wa miungu? Je, wewe ungeliambiwa utoke nje ya moto ukiwa pamoja na YESU ungelitoka?

**SIKU YA 167**
**(Juni 15)**

# Mfalme Nebukadneza Aishi Porini

**- Danieli 4**

Mfalme Nebukadreza aliamua kutoa ushuhuda wa mambo yaliyomtokea mwenyewe, kwenye kitabu cha Danieli 4. Inaonekana mfalme mwenyewe aliandika sura hii. Nimeona vema kutangaza habari za ishara na maajabu aliyonitendea Mungu aliye juu. Ishara Zake ni kubwa kama nini! Na maajabu Yake yana uweza kama nini! Ufalme Wake ni ufalme wa milele; na mamlaka Yake ni ya kizazi hata kizazi.

Nebukadreza aliendelea, akasema kuwa alikuwa amekaa katika nyumba yake ya kifahari, katika enzi yake, ndipo akaota ndoto iliyomtia hofu na kumfadhaisha kitandani mwake. Akatoa tena amri wenye hekima waletwe, akiwa ameshasahau kwamba ni Mungu tu awezaye kumfunulia ndoto yake. Basi wakaletwa tena wachawi, waganga, Wakaldayo, na wanajimu ili wamjulishe ndoto na tafsiri yake, lakini walishindwa. Basi aliingia Danieli "ambaye roho wa miungu watakatifu, inakaa ndani yake, na mfame akamwadithia ile ndoto. Mfalme akamwambia kwa kuwa miungu watakatifu wanakaa ndani yake, hapana neno la siri litakalomshinda tafsiri. Mara hii mfalme alikumbuka ile ndoto, lakini hakujua tafsiri yake. Akaeleza kuwa aliona mti katikati ya nchi, wenye urefu mkubwa, nao ukakua na kuwa na nguvu, na urefu wake ukafika mpaka mbinguni na kuonekana kwake kukaijaza dunia nzima. Majani yake yalikuwa mazuri, matunda yake mengi, na ndani yake chakula cha kuwatosha watu wote; wanyama wa kondeni nao wakapata kivuli chini yake. Ndege walikaa kwenye matawi yake, na kila kiumbe kilipata chakula pale. Katika ndoto akaona mlinzi, Naye ni Mtakatifu, akishuka toka mbinguni, Naye huyo akapaza sauti akasema, "Ukateni mti huu, yafyekeni matawi yake, yapukutisheni majani yake, na kutawanya matunda yake, wanyama na waondoke hapo chini yake na ndege katika matawi yake. Bali kiacheni kisiki cha shina lake katika ardhi, pamoja na pingu ya chuma na shaba, katika majani mororo ya kondeni; kikapate maji kwa umande wa mbinguni na sehemu yake iwe pamoja na wanyama katika majani ya nchi; moyo wake ukabadilike, usiwe moyo wa binadamu, na apewe moyo wa mnyama, nyakati saba zikapite juu yake. Hukumu hii imekuja kwa agizo la walinzi, na amri hii kwa neno la watakatifu; kusudi walio hai wapatae kujua ya kuwa Aliye juu anatawala katika ufalme wa wanadamu, Naye humpa amtakaye, tena humtawaza juu yake aliye mnyonge." Mimi Nebukadreza, nimeiona ndoto hii, na wewe Ee Belteshaza, niambie tafsiri yake, maana wenye hekima wote wameshindwa, bali wewe waweza maana roho ya miungu watakatifu inakaa ndani yako.

Ndipo Danieli akashangaa kwa muda, naye akafadhaika mawazoni, Mfalme akamwambia, "Ee Belteshaza ndoto hii isikufadhaishe wala tafsiri yake." Danieli akijua tafsiri inahusu mabaya yatakayompata mfalme, alisema kwa hekima, "ndoto hii iwapate wao wakuchukiao, na tafsiri iwapate adui zako." BWANA alimpatia

Danieli tafsiri ya ile ndoto palepale na akamwambia mfalme, "Ule mti uliouona, uliokua, ukawa na nguvu, urefu wake ukafika mpaka mbinguni, … majani yake yalikuwa mazuri, na matunda yake mengi, na ndani yake chakula cha kuwatosha wote; ambao chini yake wanyama wa kondeni walikaa, na ndege wa angani walikuwa na makao yao katika matawi yale, ni wewe! Ee mfalme, uliyekua, na kupata nguvu, maana ukuu wako umekua na kufika mpaka mbinguni, na mamlaka yako yamefika mpaka mwisho wa dunia." Yule mlinzi Mtakatifu uliyemwona akishuka na kusema ukateni mti huu na kuuangamiza, ila kiacheni kisiki na pingu hata nyakati saba zipite juu yake, "tafsiri yake ni hii, nayo ni amri yake Aliye juu, iliyomjia bwana wangu mfalme, ya kuwa utafukuzwa mbali na wanadamu, na makao yako yatakuwa pamoja na wanyama wa kondeni, nawe utalazimishwa kula majani kama ngombe, nawe utatiwa maji kwa umande wa mbinguni, na nyakati saba zitapita juu yako, hata utakapojua ya kuwa Aliye juu Ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, Naye humpa Yeye amtakaye, awaye yote. Na kwa kuwa waliamuru kukiacha kisiki cha shina lake; ufalme wako utakuwa imara kwako, baada ya wewe kujua ya kuwa mbingu ndizo zinazotawala."

Danieli akamaliza na kumpa wosia mfalme, akamwambia "Ee mfalme, shauri langu lipate kibali kwako, ukaache dhambi zako kwa kutenda haki, ukaache maovu yako kwa kuwahurumia maskini; huenda ukapata kuzidishiwa siku zako za kukaa kwa raha." Mfalme alifikiri na kuona pengine angeweza kufanya kama Danieli alivyosema, ila mali, uwezo na nguvu vikampa kiburi na kumshusha chini.

Mfalme akaendelea kujisifu kwa kiburi. Baada ya miezi 12, alikuwa akitembea ndani ya jumba la kifalme katika Babeli. Mfalme akanena akasema, "Mji huu sio Babeli mkubwa nilioujenga mimi, uwe kao langu la kifalme, kwa uwezo wa nguvu zangu, ili uwe utukufu wa enzi yangu?" Maneno hayo yalipokuwa yangali kinywani mwake, akasikia sauti ikitoka mbinguni ikisema, "Ee mfalme Nebukadreza, maneno haya unaambiwa wewe; Ufalme huu umeondoka kwako. Nawe utafukuzwa mbali na wanadamu, na makao yako yatakuwa pamoja na wanyama wa kondeni; utalishwa majani kama ng'ombe, na nyakati saba zitapita juu yako, Hata utakapojua ya kuwa Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, na humpa amtakaye, awaye yote. Saa iyo hiyo jambo hilo likatimizwa, likampata Nebukadreza; alifukuzwa mbali na wanadamu, akala majani kama ngombe, na mwili wake ulilowa maji kwa umande wa mbinguni, hata nywele zake zikakua, zikawa kama manyoya ya tai, na kucha zake kama kucha za ndege. Kweli Mungu wetu ni wa ajabu, alimpa nafasi mfalme huyu mara nyingi, kwa kumpenda, lakini akazitumia vibaya, kadhalika na sisi tusije tukarudia makosa ya mfalme huyu, tukaacha kutumia nafasi za wokovu tunazopata kwa kutubu na kuungama na kukaa upande wa Bwana.

Basi hata mwisho wa miaka saba, Nebukadneza akainua macho mbinguni na fahamu zake za ubinadamu zikamrudia, akamhimidi BWANA, na kumsifu na kumheshimu Yeye aishiye milele, kwa maana mamlaka Yake ni mamlaka ya milele na ufalme Wake toka kizazi hadi kizazi. Akatambua kuwa wote wanaokaa duniani si kitu, naye hufanya kama atakavyo katika jeshi la mbinguni, na katika hao wanaokaa duniani; wala hapana awezaye kuuzuia mkono wake, wala kumwuliza, "Unafanya nini Wewe?"

Kiburi kilimwangusha Lusifa mbinguni akapewa jina baya la Shetani (Isa. 14:12-15; Eze. 28:14-17). Wazazi wetu Bustanini Edeni walidanganywa na Shetani kuwa wakila tunda lile lililokatazwa watakuwa kama Mungu. Wakala, wakajiona uchi, wakapoteza utukufu walioumbiwa nao, na wazao wao wakawa wamepungukiwa na utukufu huo (Mwa. 3:3-7; Rum. 3:23). Mungu anachukia sana kiburi kwa sababu nafsi yetu inataka kumwondoa katika kiti Chake cha enzi mioyoni mwetu na kukikalia yenyewe na huku tukiwatesa wenzetu! (Mithali 6:16- 19). Tulijifunza katika somo la kwanza (Danieli 1) kwamba miili yetu ni Hekalu la Roho Mtakatifu. Mtu anayeiruhusu nafsi kutawala moyo wake anamfukuza Roho moyoni mwake. Kama kuna vita kali kuliko zote hapa duniani ni ile ya kupigana na nafsi yetu. Nafsi haifi kabisa; inaweza kukandamizwa tu isijitutumue. Kwa hiyo ni muhimu kuwa macho kila wakati ili isije ikajitutumua juu ya Mungu au juu ya watu wengine. Paulo alikuwa na vita iyo hiyo. Anasema, "Ninakufa kila siku" (1 Kor. 15:31). Kwa maneno mengine, "naifisha nafsi yangu kila siku," au "napigana na umimi unaojiinua ndani yangu." Kuweza kuidhibiti nafsi ni kwa njia ya kumruhusu Kristo kukaa moyoni mwetu, "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi [si umimi wangu] tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi Yake kwa ajili yangu" (Gal. 2:20). Nafsi itaondolewa ndani yetu wakati wa parapanda ya mwisho tutakapopewa miili ya utukufu, isiyokufa (1 Kor. 15:51-53). Ndiyo maana si vizuri mtu kujisifu kuwa ameokoka, maana anaweza kuangushwa na nafsi wakati wo wote na kupoteza wokovu wake (1 Kor. 10:12; Eze. 33:12-16; Mt. 24:13). Kwanza kule kujisifu kwenyewe tu ni dhambi ambayo haina msamaha mpaka mtu huyo atubu na kujishusha kiburi chake (Luka 18:9-14). Tunaruhusiwa kujisifia msalaba wa Kristo tu uliotuletea ukombozi sisi tusiostahili (Gal.6:14). Sifa zote anastahili kupewa Mungu kwa lo lote tufanyalo au kwa mafanikio yetu (Yer.9:23,24). (Mzee mwalumbili)

Mungu ni Mwenye rehema. Basi mawaziri wakaja kumtafuta na kumrudisha tena katika ufalme! Mungu Ndiye, alimrudisha katika ufalme, hakuna atakayekungoja miaka saba utembee kama ngombe kisha urudi tena uwaongoze watu. Mungu akamwongezea Nebukadreza enzi kupita aliyokuwa nayo, na Nebukadreza akatoa ushuhuda wake kwa kila mtu na kumhimidi, kumtukuza, na kumheshimu BWANA maana matendo Yake ni ya kweli, na njia Zake ni za adili, na wale waendao kwa kiburi, Yeye aweza kuwashusha au kuwadhili. Mfalme huyu mwenye uwezo, hatimaye aliona njia ya Mungu. Akakubali kuwa Mungu Ndiye Mweza, na anamiliki na kuongoza mambo yote, naye si kitu. Hata nasi leo tunaweza kujifunza kujinyenyekeza kutoka kwa mfalme huyu.

Mungu na ashukuriwe! Nebukadreza alijifunza kwa njia ya aibu sana (ya kuwa mwehu) kwa miaka saba mizima. Alitoka akiwa kiumbe kipya; akakitubia kiburi chake sugu na kuanzia hapo akaanza kumtukuza hadharani Mungu wa mbinguni (Dan. 4:34,35). Ufalme wake akarudishiwa. Ushuhuda wake mbele za watu ameutoa mwanzo wa Sura hii ya 4. "Mfalme Nebukadreza, kwa watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wanaokaa katika dunia yote; Amani iongezeke kwenu. Mimi nimeona vema kutangaza habari za ishara na maajabu, aliyonitendea Mungu aliye juu. Ishara Zake ni kubwa kama nini! na maajabu Yake yana uweza kama nini!

Ufalme Wake ni ufalme wa milele; na mamlaka Yake ni ya kizazi hata kizazi" (Dan. 4:1-3). Siku moja wale watakaookolewa watakutana na Nebukadreza mbinguni. Atawasimulia vizuri kisa chake. Ni wangapi ambao Mungu anapozungumza nao katika Neno Lake wanakaza shingo zao kwa kiburi na kuyatukuza mawazo yao juu ya Mungu na kufanya kinyume na maagizo Yake? Je, wako tayari kupelekwa porini na kula majani ili wajifunze? Hilo ni zoezi kali mno. Je! Mungu atanivumilia mpaka lini asiukate mti wangu? (Luka 13:6-9). Yatupasa kutubu; la sivyo tutaangamizwa (Luka 13:1-5). Sisi si maarufu kuliko Mungu;
wala sisi si bora kuliko wengine.

*Omba kwa ajili ya Vijana wa Kanisa — Hebu wale walio wazee katika uzoefu waangalie vijana; na wanapowaona wakijaribiwa, wawachukue kando, na waombe nao na kwa ajili yao.

---

Nani aliandika hii sura ya Danieli? Nebukadreza aliota ndoto gani? Tafsiri yake ilikuwa nini? Unaweza kuelezea mfalme alivyofanana alipokuwa kondeni kama mnyama? Kwa nini hakujizuia asijisifu ili mabaya yasimtokee? Je! kuna ubaya gani kujisifu? Kwa nini Mungu alimwongezea enzi Nebukadreza? Mtu anawezaje kuepuka hila ya kiburi?

**SIKU YA 168**
**(Juni 16)**

# Kiganja cha Mkono Kisicho na Damu Chaandika Ukutani

**- Danieli 5**



Wakati Nebukadreza alipokufa, mtoto wake, ambaye alikuwa dhaifu, aliyeitwa Evil-merodaki, alirithi ufalme, lakini alipenda kutembea nchi mbalimbali na kuishi kwa anasa, hivyo akamwachia mtoto wake, Belshaza, atawale katika mji mkuu. Baba na mwana walifanya utawala pamoja. Mfalme Belshaza alikuwa mwovu, wala hakujifunza yaliyompata babu yake, Nebukadreza. Siku moja aliamua kuwafanyia wakuu wake karamu kubwa. Alipokuwa akionja divai, akaamuru wavilete vyombo vya hekalu la Yerusalemu ambavyo babu yake alivichukua alipouhusuru Yerusalemu, ili yeye na masuria wake wapate kuvinywea, basi wakavileta vile vyombo vya dhahabu, vilivyokuwa kwenye hekalu la Mungu lililokuwako Yerusalemu, wakavinywea na kuisifu miungu ya dhahabu, fedha, shaba, chuma, miti, na mawe. Saa hiyo hiyo vikatoea vidole vya mkono wa mwanadamu bila mwili na kuandika ukutani. Mfalme alipoona kile kitanga cha mkono kinaelea chenyewe na kuandika, uso ulimbadilika na fikira zake zikamfadhaisha, viuno vyake vikalegea, na magoti yakagongana kwa kutetemeka. Mfalme akapiga yowe na kulia kwa sauti kubwa akamuru waletwe wachawi, Wakaldayo na wanajimu. Hata leo, baadhi ya watu wakiwa na shida huenda kwa wachawi na wanajimu ambao

hutumia nguvu za Shetani katika kuwatatulia matatizo yao. Hili ni kosa, imetupasa tupige magoti na kuomba dua kwa Mungu wa mbinguni. Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, na sio kwa Shetani au wafuasi wake. Mfalme akanena kwa wenye hekima akiahidi zawadi kwa yeyote atakayesoma maandiko haya na kutoa tafsiri yake. Akasema atavikwa mavazi ya kifalme ya zambarau. Kisha atapewa mkufu wa dhahabu, na kuwa mtu wa tatu katika ufalme, kwani yeye na babaye walikuwa wakitawala wakati mmoja. Basi wakaingia wenye hekima wote wa mfalme lakini wakashindwa kusoma yale maandiko na wala hawakuweza kumpa mfalme tafsiri yake.

Mfalme alipokuwa akihangaika na uso umembadilika, magoti yake yakipga makofi yenyewe, wakati akitetemeka, ile karamu ikageuzwa kuwa hofu na vilio, yeye alifikiri Mungu hai na wa Kweli anaweza kuchezewa. Alikuwa na vikombe tele, ila alitaka kumkufuru. Mungu wazi wazi kwa kutumia vile ambavyo ni vya wakfu. Babu yake Nebukadneza aliviheshimu vyombo hivi. Wakuu wakamwita malkia ambaye alimjua Danieli fika. Basi malkia, kwa sababu ya maneno ya mfalme na ya wakuu wake, akaingia katika nyumba ya karamu; malkia akanena, akasema, Ee mfalme, uishi milele; fikira zako zisikufadhaishe; wala uso wako usibadilike. Yuko mtu katika ufalme wako, ambaye roho ya miungu watakatifu inakaa ndani yake; na katika siku za baba yako nuru na ufahamu na hekima zilionekana ndani yake; na mfalme Nebukadreza, baba yako, naam, mfalme, baba yako, akamfanya kuwa mkuu wa waganga, na wachawi, na Wakaldayo, na wanajimu; kwa kuwa roho njema kupita kiasi, na maarifa, na ufahamu, na uwezo wa kufasiri ndoto, na kufunua maneno ya fumbo, na kufungua mafundo, zilionekana katika Danieli huyo, ambaye mfalme alimwita Belteshaza. Basi na aitwe Danieli, naye ataionyesha tafsiri." Ndipo Danieli akaitwa, sasa akiwa ni mtu mzima, pengine akiwa na umri zaidi ya miaka 85. "Na Mfalme akanena, akamwambia Danieli, Je! Wewe ndiwe Danieli yule, aliye mmoja wa wana wa Yuda waliohamishwa, ambao mfalme, baba yangu, aliwaleta huku toka Yerusalemu? Nimesikia habari zako, kwamba roho ya miungu imo ndani yako, na kwamba nuru na ufahamu na akili bora zimeonekana kwako. Basi sasa, watu wenye hekima na wachawi wameletwa mbele yangu, wapate kulisoma andiko hili, na kunijulisha tafsiri yake; lakini hawakuweza kunijulisha tafsiri ya jambo hili. Lakini nimesikia habari zako, kwamba waweza kuleta tafsiri, na kufumbua mafumbo; haya! Kama ukiweza kulisoma andiko hili, na kunijulisha tafsiri yake, utavikwa mavazi ya rangi ya zambarau, na kuwa na mkufu wa dhahabu shingoni mwako, nawe utakuwa mtu wa tatu katika ufalme."

Inashangaza kwamba hakuwa anamjua Danieli hata kidogo, mtu aliyefanya kazi na babu yake kwa njia ya ajabu. Danieli hakuhitaji zawadi hizo. "Ndipo Danieli akajibu, akasema mbele ya mfalme; Zawadi zako zishike wewe mwenyewe; na thawabu zako mpe mtu mwingine; walakini nitamsomea mfalme maandiko haya, na kumjulisha tafsiri yake. Kwa habari zako, Ee mfalme, Mungu Aliye juu alimpa Nebukadreza, baba yako, ufalme, na ukuu, na fahari, na utukufu; na kwa sababu ya ule ukuu aliompa, watu wa kabila zote, na mataifa, na lugha, wakatetemeka na kuogopa mbele yake; aliyetaka kumwua alimwua; na aliyetaka kumwacha hai, alimwacha hai; aliyetaka kumtukuza, alimtukuza; na aliyetaka kumshusha, alimshusha. Lakini moyo wake ulipoinuliwa, na roho yake ilipokuwa ngumu akatenda kwa kiburi, alizuliwa katika

kiti chake cha enzi, nao wakamwondolea utukufu wake. Akafukuzwa mbali na wanadamu, moyo wake ukafanywa kuwa kama moyo wa mnyama, na makao yake yalikuwa pamoja na punda-mwitu; akalishwa majani kama ng'ombe, mwili wake ukalowa maji kwa umande wa mbinguni; hata alipojua ya kuwa Mungu Aliye juu ndiye anayetawala katika ufalme wa wanadamu, na ya kuwa humweka juu yake Yeye amtakaye, awaye yote. Na wewe, mwanawe, Ee Belshaza, hukujinyenyekeza moyo wako, ijapokuwa ulijua hayo yote. Bali umejiinua juu ya Bwana wa mbingu; nao wamevileta vyombo vya nyumba Yake mbele yako; na wewe, na wakuu wako, na wake zako, na masuria wako, mmevinywea; nawe umeisifu miungu ya fedha na ya dhahabu na ya shaba, na ya chuma, na ya mti, na ya mawe; wasioona, wala kusikia, wala kujua neno lo lote; na Mungu Yule, ambaye pumzi yako i mkononi Mwake, na njia zako zote ni Zake, hukumtukuza." Akamwambia yeye, Belshaza, hakujinyenyekeza mbele za Mungu, japo alijua hayo yote.

Akasema, umejiinua kwa BWANA na umivileta vyombo vitakatifu, vilivyowekwa wakfu kwa huduma ya hekaluni. Nawe umeisifu miungu yako ya dhahabu, chuma, fedha na miti isiyoona wala kusikia, wala hukumtukuza Mungu anayekupa pumzi na kukukwezesha katika njia zako.

Ndipo kile kitanga cha mkono kikaletwa kutoka mbele zake, na maandiko yakasomwa. Nayo yaliandikwa hivi:

MENE, MENE, TEKELI, NA PERESI. Tafsiri yake mfalme ni:- MENE-Mungu ameuhesabu ufalme wako na kuukomesha.

TEKELI - umepimwa katika mizani nawe umeonekana umepunguka. PERESI-ufalme wako umegawanyika, nao wamepewa Wamedi na Waajemi. Ndipo Belshaza akatunza neno lake la kumzawadia Danieli mavazi, na mkufu. Wakapiga mbiu na kutangaza kwamba yeye ni mtu wa tatu katika ufalme. Hata hivyo, usiku ule, ulikuwa ndio wa mwisho wa ufalme wa Babeli. Wamedi na Waajemi waliingia wakipitia mtoni, maana mji ulikuwa na ukuta mkubwa na mrefu, hivyo waliweza kupita bila shida wakati watu wakiendelea na karamu yao ya uovu.

Usiku uo huo Belshaza, mfalme wa Wakaldayo, akauawa. Na Dario, Mmedi, akaupokea ufalme na umri wake ulikuwa miaka 62. Hili ni fundisho kubwa kwetu kuwa imetupasa kuwa wanyenyekevu kama Danieli na Mungu atatukweza kwa wakati wake. Tuondoe kiburi cha Belshaza cha kutomheshimu Mungu na kutoheshimu vitu vitakatifu vya kanisani au hekaluni. Bwana atusaidie ili tuheshimu mambo matakatifu. Hekalu/kanisani si mahali pa kukimbia kimbia na kuharibu vitu au kuvitumia jinsi tunavyotaka.

Hakika moyo wa mwanadamu umejaa upumbavu mwingi. "Mpumbavu amesema moyoni, Hakuna Mungu; Wametenda uovu wa ufisadi na kuchukiza, Hakuna atendaye mema"(Zab.53:1). Watu wanaopenda kufanya dhambi huamua kumfutilia mbali Mungu katika mawazo yao, mafundisho yao, na maisha yao. Biblia inasema huo ni upumbavu. Kwa sababu Mungu Yu kweli, na watu kama hao watawajibika kwa vitendo vyao viovu. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba hatujifunzi kutokana

na yale yaliyowapata watangulizi wetu. Tunataka kujionea wenyewe na tunakuwa tumechelewa.

*Walimu wa Shule ya Sabato Ombeeni Washiriki wa Darasa Lenu—Kama wafanyakazi wa MUNGU tunahitaji zaidi kuwa kama Yesu na kupunguza ubinafsi. Tunapaswa kuwa na mzigo zaidi kwa ajili ya nafsi, na tunapaswa kuomba kila siku kwamba nguvu na hekima ziweze kutolewa kwa ajili ya Sabato. Waalimu, kutaneni na madarasa yenu. Omba pamoja nao, na uwafundishe jinsi ya kuomba. Hebu moyo ulainishwe, na maombi yawe mafupi na mepesi, lakini ya dhati na bidii.

---

Belshaza alifanya dhambi gani? Ni nani alindika ukutani? Nani alisema Danieli aitwe? Unapata fundisho gani kwenye kisa hiki? MENE MENE TEKELI NA PERESI ina maana gani? Kila siku tujiulize, "Je! tukipimwa kwenye mizani ya Mungu tutakutwaje?"

**SIKU YA 169**
**(Juni 17)**

# Danieli Atupwa Kwenye Pango la Simba


**- Danieli 6**

Basi ilimpendeza Dario mfalme wa Wamedi kuweka maakida 120, na wakuu watatu wakisimamia hao maakida. Danieli hakufukuzwa au kuuawa, bali alichukuliwa na utawala mpya kuwa mmoja wa hao maakida watatu, ili maliwali hawa watoe hesabu kwao isipatikane hasara kwa mfalme. Wengine walichukia, kwamba mtu wa ufalme wa zamani apate cheo katika ufalme mpya. Sifa za Danieli zikavuma kupita maliwali wote kwa kuwa roho wa Mungu alikuwa ndani yake, naye mfalme akaazimu kumweka juu ya ufalme wote. Hili likaleta wivu kwa viongozi wengine, hivyo wakatafuta sababu za kumshtaki ili kumwangusha kwa sababu zisizo na msingi. Basi wakasemezana, wakisema, "hatutapata sababu ya kumshitaki huyo Danieli, tusipoipata katika mambo ya sheria ya Mungu wake." Danieli aliazimia kumtii Mungu, na hili ni fundisho la utii kwetu leo. "Basi wale mawaziri na maamiri wakakusanyika pamoja mbele ya mfalme, wakamwambia hivi, Mfalme Dario, uishi milele. Mawaziri wote wa ufalme, na manaibu, na maamiri, na madiwani, na maliwali wamefanya shauri pamoja ili kuweka amri ya kifalme; na kupiga marufuku, ya kwamba mtu ye yote atakayeomba dua kwa Mungu awaye yote, au kwa mtu awaye yote, katika muda wa siku thelathini, ila kwako, Ee mfalme atatupwa katika tundu la simba. Sasa, Ee mfalme, piga marufuku, ukatie sahihi maandiko haya, yasibadilike, kama ilivyo sheria ya Wamedi na Waajemi, isiyoweza kubadilika." Basi hata kabla mfalme hajafikiria vizuri, wala kujua mtego wao, akaona ni jambo jema yeye kutukuzwa, asijue ni mtego kwa rafiki yake mpendwa, Danieli. Mfalme akaambiwa papo hapo aweke sahihi na muhuri wake kwenye maandiko hayo ambayo tayari walikuwa wamekwisha kuandika, ili yasibadilishwe kama ilivyo sheria ya Wamedi na Waajemi, isiyoweza kubadilika. Wakisema kitu ni lazima kifanyike kama ilivyotamkwa.

Hata Danieli, alipojua kuwa ile sheria imekwisha kutiwa muhuri na mfalme, akaingia nyumbani mwake na madirisha katika chumba chake yalikuwa yamefunguliwa kukabili Yerusalemu, kisha akapiga magoti na kusali mara tatu kwa siku kukabili Yerusalemu kama Wayahudi walivyofanya, akimshukru Mungu wake kama alivyofanya awali, asibadilishe mambo kutokana na hali halisi.

Wale viongozi, mawaziri na maliwali wakakusanyika na kumwona akiomba dua, ili wapate ushahidi. Kisha wakasema, Je! hakutilia maanani sahihi ya mfalme, kwamba siku hizi thelathini aombe dua kwa mfalme Dario tu, la sivyo atatupwa tunduni mwa simba? "Ndipo wakakaribia, wakasema mbele ya mfalme katika habari ya ile marufuku ya mfalme; Je! Hukuitia sahihi ile marufuku, ya kwamba kila mtu atakayeomba dua kwa Mungu awaye yote, au kwa mtu awaye yote, katika muda wa siku thelathini, ila kwako, Ee mfalme, atatupwa katika tundu la simba? Mfalme akajibu, akasema, Neno hili ni kweli, kama ilivyo sheria ya Wamedi na Waajemi

isiyoweza kubadilika. Basi wakajibu, wakasema mbele ya mfalme, Yule Danieli, aliye mmoja wa wana wa wale waliohamishwa wa Yuda, hakujali wewe, Ee mfalme, wala ile marufuku uliyoitia sahihi, bali aomba dua mara tatu kila siku." Danieli alikuwa mtu wa tabia njema, maana hakusema aombe akijificha akingoja siku thelathini zipite, aliona atakuwa amemkosea Mungu wa mbinguni, Mwenye kustahili utukufu na aliyemtoa mbali, hata hivyo, taifa hili lisilomjua Mungu vizuri watajifunzaje?
Mfalme akashituka, na kukasirika, ndipo aligundua mtego wa wale waovu, akatafuta njia ya kumwokoa Danieli na ile sheria yao isiyobadilika, akahangaika, mpaka jua likachwa, lakini akashindwa. Ndipo wale viongozi wakafurahi kuona kuwa Danieli ataangamia. Wakamkazania na kumkumbusha mfalme kwamba sheria yao haibadiliki. Basi mfalme akatoa amri wamlete Danieli, naye akampa maneno ya mwisho ya kumtia moyo, "Danieli, Mungu wako unayemtumikia daima, yeye atakuponya," Umati ukashuhudia mzee Danieli akitupwa tunduni mwa simba. Siku hizo walifuga simba, na walitupa watu wabaya na wema kutegemeana na mfalme aliyekuwa madarakani, kama ni mbaya au mwema. Baada ya Danieli kutupwa ndani ya shimo hilo lililokuwa na simba kadhaa, likaletwa jiwe, likawekwa mdomoni mwa tundu, naye mfalme akalitia muhuri wake mwenyewe kama wakuu walivyomtega, na wakafikiri wamemweza mfalme na rafiki yake.



Mfalme alienda nyumbani kwake, lakini usiku kucha hakupata usingizi, akijua kuwa Danieli hana hatia na wale viongozi wamefanya njama tu za kumwangamiza. Mfalme huyu alifunga, na usiku ule vinanda havikuletwa ili kumtumbuiza, usingizi ukampaa. Kulipopambazuka, mfalme akaharakisha kwenda penye tundu la simba, na alibokaribia pale alimlilia Danieli kwa sauti ya huzuni. Kisha akamwita Danieli "Danieli, Ee Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, Je! Mungu wako, unayemtumika daima, aweza kukuponya na simba hawa?" Ndipo moyo wake ukafarijika sana aliposikia sauti ya Danieli, "Ndipo Danieli akamwambia mfalme, Ee mfalme, uishi milele. Mungu wangu amemtuma malaika Wake, naye ameyafumba makanwa ya simba, nao hawakunidhuru; kwa kuwa mbele Zake mimi nalionekana kuwa sina hatia; tena, mbele yako, Ee mfalme, sikukosa neno. Basi mfalme akafurahi sana, akaamuru wamtoe Danieli katika lile tundu. Ndipo Danieli akatolewa katika lile tundu, wala dhara lo lote halikuonekana mwilini mwake, kwa sababu alikuwa anamtumaini Mungu wake." Simba wenye njaa walitembea usiku mzima matumbo yakinguruma, bali hawakumgusa nabii wa Mungu. Viongozi wakiwa wamenuna, maana ajenda yao haijafanikiwa, Danieli alitolewa, hakuwa na dhara lolote, mwilini mwake kwa sababu alimtumaini Mungu wake. Alishinda mtihani mara nyingine, akiwa mzee wa miaka mingi.

Mfalme akaamuru wote waliomshtaki Danieli waletwe, mfalme akaamuru watupwe wale watu kwenye tundu la simba, wao, watoto wao na wake zao, na wale simba wakavamia na kuvunja mifupa yao vipande vipande kabla ya kufika chini maana walikuwa wamenyimwa chakula ili wamle Danieli, bali wakaliwa wao. Mtu akichimba shimo kudhuru wengine, mwishowe atadumbukia yeye mwenyewe.

Ndipo mfalme Dario, akastaajabu na kuandika waraka kwa taifa lote, kwa lugha za nchi mbalimbali za milki aliyotawala, "Amani na iongezeke kwenu. Mimi naweka amri, ya kwamba katika mamlaka yote ya ufalme wangu watu watetemeke na kuogopa mbele za Mungu wa Danieli; maana Yeye Ndiye Mungu aliye hai, adumuye milele, na ufalme Wake ni ufalme usioharibika, na mamlaka yake itadumu hata mwisho. Yeye huponya na kuokoa, hutenda ishara na maajabu mbinguni na duniani, Ndiye aliyemponya Danieli na nguvu za simba." Yaani, mfalme alihubiri kwa wote katika ufalme wake na kuwaeleza matendo makuu ya Mungu. Hata leo katika nafasi yako, unapaswa kutoa ushuhuda wa matendo makuu ya Mungu. Kumsifu Mungu ni sadaka pia.
Basi Danieli alifanikiwa sana katika enzi ya Dario Mmedi na katika enzi ya Koreshi Mwajemi.

Hata sisi leo, tutafanikiwa kama tunamtukuza Mungu wetu tukifuata maagizo Yake, Yeye Mwenyewe atatukweza. Wahenga walisema, "Mchimba shimo hutumbukia mwenyewe." Biblia inasema, "Mwenye kuchimba shimo atatumbukia ndani yake" (Mhu. 10:8). Siku zile za Esta Hamani akamwonea wivu au kijicho Mordekai. Kwa siri akachonga mti mrefu sana wenye ncha kali wa kumtundikia Mordekai, mtu wa Mungu aliyekuwa hana hatia yo yote kama Danieli. Matokeo? Alitundikwa mwenyewe kwenye mti ule ule aliouchonga kwa mikono yake (Esta 7:9,10). Hebu tuwe watu wenye upendo na sio wenye kuwachimbia watu wengine mashimo na kisha tukadumbukia wenyewe.

*Wanafunzi waombe kwaajili ya Walimu-Wanafunzi wanapaswa kuwa na nyakati zao za maombi, ambapo wanaweza kutoa maombi ya kudumu, marahisi ili MUNGU ambariki rais wa shule kwa nguvu za mwili, akili timamu, nguvu ya maadili, na utambuzi wa kiroho, na kwamba kila mwalimu astahili kwa neema ya MUNGU kufanya kazi yake.

---

Kwa nini watu walitaka Danieli atupwe kwenye tundu la simba? Kwa nini mfalme alisikitika? Mungu alimwokoaje Danieli? Ni nini kilitokea wakati wale watu waovu walipotupwa kwenye tundu la simba? Kwa nini Danieli alifanikiwa sana katika enzi ya Dario Mmedi na Koreshi Mwajemi? Kumsifu Mungu ni sadaka, Je! wewe unamsifu? Je! Siku za mwisho mateso kwa watu wa MUNGU yatarudia?

**SIKU YA 170**
**(Juni 18)**

# Wanyama wa Ajabu

**- Danieli** 7



Katika mwaka wa kwanza wa kumiliki mfalme Belshaza Danieli aliota ndoto na maono yake aliyoona kitandani mwake, akayaandika, na kutoa habari ya mambo hayo yote. Aliona wakati wa usiku pepo nne za mbinguni zikivuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa, kisha wanyama wakubwa wanne, wakatoka baharini, wote wa namna tofauti.

Wa kwanza alikuwa kama simba, mwenye mabawa ya tai, halafu mabawa yake yakafutuka manyoya, kisha akainuliwa katika nchi na kusimamishwa juu kwa miguu miwili kama mwanadamu; naye akapewa moyo wa kibinadamu. Kisha akatazama na mnyama wa pili alikuwa kama dubu, naye aliinuliwa upande mmoja, na mifupa mitatu ya mbavu ilikuwamo kinywani mwake katika meno yake; wakamwambia mnyama huyo, "inuka, ule nyama tele."

Kisha akatazama na mnyama mwingine kama chui, ambaye juu ya mgongo wake alikuwa na mabawa kama ya ndege, na vichwa vinne, akapewa mamlaka.

Kisha katika hiyo njozi ya usiku, aliona mnyama wa nne mwenye kutisha, mwenye nguvu na uwezo mwingi, naye alikuwa na meno makubwa sana ya chuma. Alikula na kuvunja vipande vipande na kukanyaga mabaki kwA miguu yake, na umbo

lake lilikuwa tofauti kabisa na wale wa kwanza. Alikuwa na pembe kumi, nyingine ikazuka kati yao, nayo ilikuwa ndogo, ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza zikangolewa kabisa na tazama katika ile pembe ndogo mlikuwa na macho ya mwanadamu, na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu.

Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa na mmoja aliye mzee wa siku ameketi tayari kwa hukumu, mavazi Yake yalikuwa meupe kama theluji na nywele za kichwa Chake kama sufu safi. Kiti Chake cha enzi kilikuwa miali ya moto na gurudumu zake moto uwakao. Mto ukapita mbele Yake na maelfu elfu wakamtumikia na mamilioni wakasimama mbele Yake. Hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa. Kisha akaona mmoja mfano wa wanadamu, akaja na mawingu ya mbinguni na akamkaribia Mzee wa siku, Naye akapewa mamlaka na utukufu na ufalme kwa kabila, lugha, jamaa; na mataifa yote watamtumikia milele na milele, na ufalme Wake hautapita kamwe.

Danieli alifadhaika na haya maono, na akaomba kuuliza maana au tafsiri yake, naye akaambiwa atajulishwa. Mungu hataki watu wake wawe gizani kuhusu ufalme huu, japo kwa sasa ulimwengu unauinua juu sana. Hatimaye utakapotawala kama alivyoruhusu Mungu itakuwa kwa maangamizi ya ulimwengu mzima na dunia itafikia mwisho wake (Ufu. 17:8- 11; 6:14-17; 19:11-21). Watakatifu watakwenda mbinguni kutawala pamoja na Yesu kwa miaka 1000 (1The. 4:16,17(18); Ufu. 20:4). Dunia hii itakuwa imeharibika vibaya katika Asomaye Na Afahamu - kipindi chote cha miaka 1000 (Yer. 4:23-27). Baada ya kwisha miaka 1000 watakatifu watarudi hapa pamoja na Mji Yerusalemu Mpya (Ufu. 21:10). Ndipo waovu watakapofufuliwa na kujaribu kuuteka Mji Yerusalemu Mpya au Kambi ya Watakatifu. Moto utawala (Ufu. 20:7-10,15). Hiyo ndiyo Jehanum au Ziwa la Moto au Mauti ya Pili (Ufu. 20:14). Jehanum haiwaki sasa. Itawaka baada ya miaka ile 1000 kwisha. Watakaoingia humo watateketezwa na kuwa majivu pamoja na Shetani na malaika zake (Mal. 4:1-3; Eze. 28:14-19). Hawatafufuliwa tena milele! Ndipo watakatifu watakapoirithi nchi mpya (Ufu. 21:1; Mt. 5:5; 2 Pet. 3:10-13; Zab. 37 yote).

*Wazazi wawaombee Watoto Wao—MUNGU ameahidi kuwapa hekima wale wanaoomba kwa imani, Naye Atafanya kama vile Yeye alivyosema. Yeye Anapendezwa na imani inayomuendea kupitia Neno Lake. Mama Augustine aliomba kwa ajili ya uongofu wa mwanaye. Hakuona ushahidi wowote kwamba Roho wa MUNGU alikuwa akiushawishi moyo wake, lakini hakuvunjika moyo. Aliweka kidole chake kwenye maandiko, akiwasilisha mbele za MUNGU Maneno Yake Mwenyewe, na kusihi kama mama awezavyo kusihi. Kujidhili kwake kwa dhati, kusihi kwake kwa bidii bila ya kuchoka, imani yake isiyoyumbayumba, ilishinda, na Bwana akampa haja ya moyo wake. Hata hivi leo Yuko tayari kusikiliza maombi ya watu Wake. "Mkono Wake si mfupi hata usiweze kuokoa wala sikio Lake si zito hata lisiweze kusikia"; na wazazi wakikristo wakimtafuta kwa bidii, Yeye atajaza vinywa vyao hoja, na, kwa ajili ya Jina Lake, atafanya kazi kwa nguvu kwa ajili yao katika wongofu wa kwa watoto wao.

---

Kwanini Daniel alifadhaika? Mnyama wa Kutisha kupita wote ni nani? MZee wa siku ni nani.

**SIKU YA 171**
**(Juni 19)**

# Tafsiri ya Ndoto ya Danieli 7

Danieli akaambiwa kwamba hawa Wanyama wakubwa wanne watakaotokea duniani ni mataifa tofauti yatakayotawala mpaka mwisho wa dunia. Unabii huu ni sawasawa kabisa na ule wa Danieli 2 unaohusu sanamu ya madini. Unabii huu unathibithishwa na historia. Ufalme wa Babeli ndio ulikuwa ukitawala wakati Danieli alipopata ndoto hii. Falme zingine zilikuja miaka ya baadaye, baada ya Danieli kupata haya maono. Unabii huu wa Danieli ni muhimu sana kama ulivyo unabii wote, maana ukiusoma vizuri utajua kwamba uko katika kipindi cha historia ya dunia. Kwenye ile sanamu ya madini, kwa sasa tuko kwenye vidole vya udongo na chuma. Na kwenye hii njozi ya Danieli saba, sasa tuko katika utawala wa zile pembe kumi za Ulaya.

Tafsiri ya ndoto: kichwa cha dhahabu cha sanamu aliyoiona mfalme Nebukadreza katika Danieli 2, ni sawa na simba au utawala wa Babeli chini ya Nebukadreza na wengine waliofuata. Babeli ilitawala dunia yote iliyojulikana siku zile kwa miaka sabini, yaani, kuanzia 606 KK mpaka 539 KK. Kumbuka miaka ya kabla ya Kristo inarudi kinyume nyume.

Kifua na mikono ya fedha ni sawa na dubu mwenye mbavu tatu katika Danieli 2, ni utawala wa Wamedi na Waajemi. Zile mbavu tatu zinawakilisha nchi za Misri, Babeli na Lydia zilizopigwa na Uajemi na kushindwa. Kuinuka dubu upande mmoja kuna maana kwamba ufalme wa Waajemi ulikuwa na nguvu kuliko ule wa Wamedi. Chini ya Dario Mmedi na Koreshi Mwajemi na wafalme wengine waliotawala dunia nzima iliyojulikana wakati ule kuanzia mwaka 539 KK mpaka 331 KK.



Lile tumbo na mapaja ya shaba ya ile sanamu aliyoiona mfalme Nebukadreza, ni sawa na yule chui mwenye vichwa vinne, ambao ni ufalme wa Uyunani, uliotawala kuanzia mwaka 331 KK mpaka 168 KK. Chini ya Alexander

mkuu wa Makedonia, Ugiriki ilitawala dunia yote iliyojulikana wakati huo. Angalia vitabu vya Historia kuthibitisha. Alexander mkuu, aliyekuwa kiongozi wa ufalme wa Uyunani, alikufa akiwa na miaka 32 kwa ulevi na ufalme wake uligawanyika katika falme nne, na majemadari wake waitwao Lysimachus, Cassander, Seleucus, na Ptolemy ndiyo waliotawala. Ndiyo maana ya yule chui mwenye vichwa vinne.

Ile miguu ya chuma ya sanamu aliyoiona Nebukadneza, ni sawa na yule mnyama wa kutisha sana, ambayo anawakilisha utawala wa Kirumi, uliotawala dunia yote, baada ya kuchukua ufalme toka kwa Wayunani kuanzia mwaka 168 KK mpaka 476 KK.

Vile vidole kumi vya nusu udongo wa mfinyazi na nusu chuma, ni falme za ulaya zilizogawanyika kutoka Rumi, na kutawala dunia yote. Katika Danieli 7, hizi ni pembe kumi alizoona Danieli kutoka kwa yule mnyama wa kutisha. Nchi hizi za ulaya zilianza kutawala mwaka 476 mpaka leo na zilitawala dunia nzima, kwa makoloni yao. Wakati fulani Uingereza ilijitapa kuwa "jua la Mwingereza halitui," kwa kuwa walitawala mahali pengi duniani kama vile Canada, Jamaica, Tanzania, New Zealand, Hongkong, Australia; yaani walikuwa wana makoloni kila bara.

Baada ya haya alisema aliona pembe ndogo, ikaangusha pembe tatu kati ya zile kumi, ikafanya vita na kuwatesa watakatifu na kuwaua kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwatupa kwa simba wenye njaa. Nabii Danieli alioneshwa kuwa japo Rumi itawadhoofisha watakatifu wa Mungu, na kubadili majira na sheria, lakini siku moja utawala wake utakoma. "Hukumu yake itawekwa na mamlaka yake yataondolewa na Mungu ataleta ufalme Wake wa milele, na wengi watamtumikia na kumtii. Kama vile lile jiwe lilivyoipiga miguu ya ile sanamu aliyoiona Nebukadreza na kuleta ufalme wake, ndivyo ambavyo yule mnyama wa mwisho au ufalme wa mwisho hautakaa milele na milele.

Soma tena huu unabii katika Biblia kwa undani na umwombe Mungu akufunulie zaidi upate kuuelewa maana Mungu anataka tuujue. Danieli 2 na 7 ziko wazi kueleweka, kwa maana Danieli mwenyewe anatafsiri maana yake, kwamba ni falme zitakazotawala baadaye. Mengine tunaweza tusielewe, lakini machache yako wazi, mfano ni falme zitakazotawala mpaka mwisho wa wakati.

Watakatifu, au watu wa Mungu walioishi maisha ya utauwa wataupokea ufalme, na kuumiliki huo ufalme milele na milele.

Danieli alitaka sana kujua hasa kuhusu yule mnyama wa nne, aliyekuwa wa ajabu, na wa kutisha, aliyekuwa na meno ya chuma, makucha ya shaba, na alikula na kuvunja vunja vipande na kukanyaga mabaki kwa miguu yake. Na ile pembe yenye macho, iliyonena makuu na kuonekana hodari kuliko wenzake, kisha ikafanya vita na watakatifu na kuwashinda. Kisha akaja mzee wa siku, Mungu Baba, nao watakatifu Wake wakapewa hukumu, na majira yakawadia watakatifu waumiliki ufalme. Danieli akaambiwa, ule ufalme wa nne ndio wa mwisho na utatawala dunia nzima.

*Omba kwa ajili ya Wakristo Wenzako—Mara nyingi sana tunasahau kwamba watenda kazi wenzetu wanahitaji nguvu, faraha na uchangamfu. Katika nyakati za wasiwasi fulani na mzigo, kuweni makini kuwahakikishia kujali kwenu na huruma. Wakati mnapojaribu kuwasaidia kwa maombi yenu, wajulishe kwamba mnafanya hivyo. Muambatanishe ujumbe wa MUNGU kwa wafanyakazi Wake: "Iweni hodari na moyo wa ushujaa.

---

Yule simba aliwakilisha ufalme gani ulioitawala dunia? Yule dubu aliwakilisha taifa gani? Yule chui aliwakilisha taifa gani? Yule mnyama wa kutisha aliwakilisha taifa gani lililotawala dunia? Pembe inawakilisha nini? Vichwa vinne vya chui viliwakilisha gani?

**SIKU YA 172**
**(Juni 20)**

# Maono ya Kondoo Mume na Beberu

**- Danieli 8**

Katika mwaka wa tatu wa kumiliki kwake Belshaza, mfalme wa mwisho wa Babeli, Danieli aliona maono tena huko Shushani ngomeni, karibu na mto wa Ulai. Alipoinua macho yake mbele ya mto, aliona na tazama kondoo mume mwenye pembe mbili na pembe zile mbili zilikuwa ndefu, lakini moja, ilikuwa ndefu kuliko ya pili, na ile iliyokuwa ndefu zaidi ilizuka mwisho. Akamwona huyo kondoo mume, akisukuma upande wa magharibi, na upande wa kaskazini na upande wa kusini. Wala hakukuwa na mnyama aliyeweza kusimama mbele yake, alitenda alivyopenda akijitukuza nafsi yake. Akiwa anafikiri, ni nini kinachoendelea, akaona beberu, yaani mbuzi dume, aliyekuwa na pembe moja kubwa, naye akamwendea huyo kondoo mwenye pembe mbili, aliyekuwa akisimama kwenye mto, akamshambulia kwa ghadhabu za nguvu zake, akamwonea hasira kali, akampiga na kuvunja pembe zake mbili na huyo kondoo mume alikuwa hana nguvu za kusimama mbele yake, wala hakuna aliyeweza kumsaidia yule kondoo mume. Yule beberu akajitukuza, akawa na nguvu, na alipokuwa na nguvu, pembe yake hiyo moja ilivunjika, badala yake zikazuka pembe nne mashuhuri. Katika pembe hizo nne, ilitokea pembe ndogo iliyokua sana. Ilikua na kulifikia jeshi la mbinguni, ikaangusha chini baadhi ya jeshi lile, na ya nyota, ikazikanyaga. Naam, ikajitukuza hata juu yake aliye mkuu wa jeshi hilo, ikamwondolea sadaka ya kuteketezwa ya daima, na mahali pa Patakatifu pake pakaangushwa chini. Na jeshi likatolewa kwake pamoja na sadaka ya kuteketezwa ya daima, kwa sababu ya makosa; nayo ikaiangusha kweli hata chini;



ikatenda ilivyopenda, na kufanikiwa. Danieli akauliza, Haya maono katika habari ya sadaka ya kuteketezwa ya daima, na lile kosa lifanyalo ukiwa, yataendelea hata lini, kukanyagisha patakatifu na jeshi? Akaambiwa “Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu ndipo patakatifu patakapotakaswa.” Huu ndio unabii mrefu katika Biblia kati ya unabii wote nyakati maalumu, unabii wa siku 2300.

Danieli alitafuta kujua maana ya yale maono. Gabrieli aliamuriwa amweleweshe, naye Gabrieli akasema, “Fahamu Ee mwanadamu, kwa maana maono haya ni ya wakati wa mwisho.” Alipomtokea, Danieli alishikwa na usingizi, lakini aliamshwa. Akaambiwa kuwa yule kondoo mume ni wafalme wa Umedi na Uajemi. Kwa hiyo madini ya fedha kwenye sanamu aliyoona Nebukadreza katika Danieli 2, dubu wa Danieli 7, na kondoo mume ni kitu kimoja, yaani, ufalme wa Umedi na Uajemi. Halafu Danieli akaambiwa kuwa yule beberu ni ufalme wa Uyunani au Ugiriki, na ile pembe kuu ni mfalme wa Uyunani, yaani, Alexander mkuu, toka Makedonia aliyetwaa ufalme toka kwa Wamedi na Waajemi. Ufalme wake ulipokoma, majemedari wake wanne wakagawanya ufalme wake katika sehemu nne za kiutawala.

Danieli akaendelea kuambiwa kuwa baada ya pale atakuja, “mfalme mwenye uso mkali, afahamuye mafumbo. Nguvu zake zitakuwa nyingi mno, lakini si kwa uwezo wake mwenyewe, naye ataharibu kiasi cha kustajaabisha, na kufanikiwa na kutenda apendavyo, naye atawaangamiza watu hodari na watakatifu. “Atajitukuza mkononi mwake … naye atasimama ili kushindana naye aliye mkuu wa wakuu, lakini atavunjika bila kazi ya mikono.” Wakati ni mwaka mmoja, yaani siku 360, nyakati mbili ni siku 360 x 2=720, na nusu wakati ni siku 180, jumla siku 1260. Unabii huu unafanana na ule wa Ufunuo, na siku hizo au miaka hiyo 1260 imekwisha kupita. Rumi ilibadilisha mambo hata kuanza kwa siku kukawa saa sita ya usiku badala ya jioni kama ilivyokuwa uumbaji.

Danieli akaambiwa maono hayo maana ni ya wakati wa mwisho, baada ya siku nyingi. Danieli akazimia maana yalimtisha haya. Kisha akaugua siku kadhaa wa kadha, kisha akaondoka na kufanya shughuli zake kwa mfalme, akiendelea kustaajabia yale maono, ila hakuna aliyefahamu. Leo imepita miaka mingi toka aone maono haya, na falme hizi zimepita zote, tunachongojea ni ufalme wa Mungu, yaani, aliye mkuu wa wakuu alete ufalme wake na avunje zile falme zingine kwa “kazi isiyo ya mikono.” Mungu karibu anatimiza unabii huu kwa kumleta Yesu Kristo mara ya pili duniani ili kuhitimisha falme za ulimwengu huu na kuwachukua wateule Wake katika ufalme Wake, jiandae pamoja na nami.

Kwa kurudia Siku 2300 za Dan. 8:14 ni siku za unabii, ni sawa na miaka 2300 (Eze. 4:6). Zilianza kuhesabiwa wakati ule amri ya kuujenga upya Yerusalemu ilipotolewa mwaka 457 K.K. na kukoma 1844 B.K. Kutakaswa kwa Patakatifu ni kazi ya Hukumu au Utakaso au Upatanisho aliyoanza kufanya Kristo mwaka 1844 katika chumba cha pili cha Hekalu la mbinguni kinachoitwa Patakatifu pa Patakatifu (Ebr. 9:23-26; Ufu. 11:19). Akimaliza atatamka maneno ya kutisha sana yatakayoamua umilele wa kila mmoja wetu, ama kwa uzima wa milele, ama kwa mauti ya milele (Ufu.22:11,12). Ndipo atakuja kuwachukua watu Wake na kuwaangamiza waovu. Somo la Patakatifu ni pana sana. Unashauriwa kusoma kitabu cha Pambano Kuu,

Sura ya 24 na 25 kwa maelezo ya kutosheleza.

*Omba kwa ajili ya Waumini Wenzako—Mara nyingi sana tunasahau kwamba watenda kazi wenzetu wanahitaji nguvu, faraha na uchangamfu. Katika nyakati za wasiwasi fulani na mzigo, kuweni makini kuwahakikishia kujali kwenu na huruma. Wakati mnapojaribu kuwasaidia kwa maombi yenu, wajulishe kwamba mnafanya hivyo. Muambatanishe ujumbe wa MUNGU kwa wafanyakazi Wake: "Iweni hodari na moyo wa ushujaa."

---


Kondoo mume aliwakilisha ufalme gani?  Kwa nini alikuwa na pembe moja ndogo na moja kubwa? Beberu aliwakilisha ufalme gani? Kwa nini ile pembe ilikatika? Kwa nini Danieli alizimia? Elezea baada ya kusoma Biblia kuhusu sura hii inavyohusiana na hukumu ya mwisho.

**SIKU YA 173**
**(Juni 21)**

# Danieli Azidi Kufunuliwa Siri za Unabii

**- Danieli 9**

Tutajaribu kusema kwa urahisi ili kila mtoto aelewe japo kidogo. Unabii mwingi wa Biblia unaposema siku, una maana siku 1 ni sawa na mwaka 1. Soma Hesabu 14:34 na Ezekieli 4:6. Bahari ina maana watu wengi. Nchi kavu watu wachache. Kama una shauku ya kujua unabii zaidi basi fanya bidii ya kusoma Biblia na vitabu vya roho ya unabii. Biblia inajitafsiri yenyewe. Sasa, kwa kuwa tunaishi wakati wa mwisho, tunaweza kuangalia historia na kuona mambo kadha wa kadha. Watu kama wale wa huduma za amazing Discovery, Morning Star Radio, mahubiriTv au Amazing facts wanasaidia watu kusoma unabii waweza kuangalia Zaidi kwa kubofya google majina hayo.



Katika mwaka wa kwanza wa mfalme Dario Mmedi, mwaka ambao Wababeli walitoka kwenye ufalme, Danieli kwa kuvisoma vitabu alipata ufahamu wa ile miaka 70 iliyokuwa imenenwa ili kuutimiza ukiwa wa Yerusalemu. Yerusalemu ilikuwa imekaa ukiwa kwa miaka 70. Nabii Yeremia alikuwa ametabiri juu ya miaka hii 70 ya ukiwa wa Yerusalemu. Danieli akaomba na kusali, akielekeza uso wake kwa BWANA, akifunga na kuvaa magunia na kujipaka majivu. Akaomba msamaha kwa Mungu, "Ee Mungu mkuu kwenye kutisha, ashikaye maagano, na rehema kwao wampendao na kuzishika amri Zake, tumefanya dhambi, na ukaidi, tumetenda uovu, tumeasi, na kuacha maagizo Yako na hukumu, wala hatukuwasikiliza watumishi Wako manabii ambao walisema na wafalme wetu." Danieli alikuwa anaomba kwa niaba ya watu wake wote. Aliungama dhambi za taifa lake. Akakiri kuwa BWANA ni Mwenye haki, lakini wao wamejitia aibu kwa kumwasi BWANA, au kutotii sauti Yake. Akaungama kwamba wote wamehalifu sheria, na kugeuka, na hivyo laana imewapata kama vile mtumishi wa Mungu Musa alivyoandika katika Kumbukumbu la Torati … Danieli akaomba fadhili za Mungu, ili wageuke na kuacha uvovu. "Ee BWANA, nakusihi hasira Yako na ghadhabu zigeuzwe ili ukumbuke Yerusalemu na mlima Wako mtakatifu … Yasikilize maombi yetu, ukatazame ukiwa wetu, mji ule ulioitwa kwa Jina Lako, kwa sababu ya rehema zako nyingi, utusamehe, usikawie."

Akiwa katika kuomba na kuungama dhambi mbele za Mungu, malaika Gabrieli

akamtokea tena. Akasema, "Nimetokea ili nikupe akili upate kufahamu…maana wewe unapendwa sana."

Malaika akamwambia kuwa muda wa majuma sabini ulikuwa umeamriwa kwa watu wake, na juu ya mji Wake mtakatifu ili kukomesha makosa na kuishiliza dhambi, na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu na kuleta haki ya milele, na kutia muhuri maono na unabii, na kumtia mafuta Yeye aliye mtakatifu. Akaambiwa, "Basi ujue na kufahamu ya kuwa tangu kuweka amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake masihi aliye mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake…katika wakati wa taabu. Na baada ya yale majuma sitini na mawili, Masihi atakatiliwa mbali, Naye atakuwa hana kitu; na watu wa mkuu atakayekuja watauangamiza mji, na patakatifu; … Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; na kwa nusu juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu; na mahali pake litasimama chukizo la uharibifu; na hivyo, hata ukomo, na ghadhabu iliyokusudiwa imemwagwa juu yake mwenye kuharibu."

Wakristo wa mataifa mbalimbali wanaitwa "Wayahudi" au "Waisraeli" wa Kiroho (Rum. 2:28,29; 9:6-8; Gal. 3:26-29). Kifo cha Yesu msalabani kilifutilia mbali tofauti iliyokuwapo kati ya Wayahudi na Mataifa; wote sasa wako sawa na wana haki sawa kwa njia ya kumwamini Kristo (Efe. 2:11-22). Tungepiga kelele na kusema, "Bwana asifiwe!!!".Hakuna tofauti tena. Chini ya Msalaba ule wa Kalvari wanadamu wote ni sawa. Hakuna haja ya kuwatengea kipindi maalum cha kuwahubiri injili Wayahudi. Wanapaswa kuhubiriwa injili sasa; siku ya wokovu kwa kila mwanadamu ni sasa, sio baada ya kanisa kunyakuliwa (2 Kor. 6:2). Kulinyakua kanisa kutaambatana na kuangamizwa kwa yule Chukizo la Uharibifu na wote wanaomwunga mkono (Dan. 9:27; Ufu. 19:11-21). MUNGU atusaidie kuwa upande Wake daima.

*Tunapaswa kuomba kwa MUNGU zaidi ya tunavyoomba. Kuna nguvu nyingi na baraka katika kuomba pamoja katika familia zetu, kuomba pamoja na watoto wetu na pia kuwaombea tukiwa wenyewe. Hebu Kristo akupatie mkono Wake wa msaada ili kutekeleza makusudi Yake. Kwa maombi unaweza kupata uzoefu ambao utafanya huduma yako kwa watoto wako iwe na mafanikio kamili.


---

Kwa nini ni muhimu kuomba kwa ajili ya watu wengine? Kwa nini Danieli alisema wamekosa wote japo yeye hakukosa? Kwa nini ni muhimu kusoma unabii wa Danieli? Je, hata wewe unaweza kuomba ili uelewe unabii wa miaka 2300? Majuma sabini ni siku ngapi?

**SIKU YA 174**
**(Juni 22)**

# Unabii wa Siku 2300 Wafunuliwa

**- Danieli 9**





Wafalme watatu walitoa amri ya kuujenga upya Yerusalemu, nao ni Koreshi, Dario na Artashasta. Mbiu ya mwisho ilikuwa mwaka 457 KK. Majuma 69 ni sawa na siku 483 na kwa unabii, siku moja ni mwaka mmoja, hivyo ukifanya hesabu, unabii huu ulianza mwaka 457 KK, na unapata mwaka 27 BK, mwaka huo ndio Yesu alibatizwa, yaani, "Masihi kutiwa mafuta."

(Angalia chati hapa uweze kuona vyema)

Mwaka 457 KK (-457) – Mwanzo wa siku/miaka 2300 na majuma 70, ilipotolewa amri ya mwisho ya kuujenga upya mji wa Yerusalemu – Ezra 7:1-27

Mwaka 27 BK – Mwisho wa majuma 69; Masihi atiwa mafuta – Kristo alibatizwa- Danieli 9:26. Mwaka 31 BK – Katikati ya juma, juma la sabini – Kristo asulubiwa- Danieli 9:26, 27.
Mwaka 34 BK – Mwisho wa majuma sabini- Stefano apigwa mawe – Matendo 7:59.




Mwaka-457+ miaka 2300=Mwaka 1843 ambao walipofanya mahesabu ya Pasaka na mengineyo walifikia tarehe ya Oktoba 22, 1844. Watu katika miaka hii huko Ulaya, Amerika na waliposoma Biblia walifikiri ina maana kwamba YESU anarudi mwaka huo maana walisema Hekalu sasa lipo mbinguni na si duniani. Mahesabu yalikuwa sawa ila tukio lenyewe lilikuwa kule mbinguni kuanza hukumu, kwa wale ambao wamekufa kwanza. Kisha baadaye kwa walio hai, na hivyo utakuwa mlango umefungwa kwa watu kutubu na kuomba msamaha. Waebrania nane, tisa na kumi yaelezea Zaidi hekalu hili la mbinguni, na kwamba lile la duniani la Kutoka 25 lilikuwa kivuli au mfano wa lile la mbinguni.

Mlango wa Rehema hufungwa kwanza kwa watu ambao wamepata nafasi ya kumjua MUNGU kwanza (watu wa nyumba ya MUNGU).

Tunapanga kuandika kidogo kitabu kuhusu unabii ili kuelezea Zaidi kwa machache tunayoelewa, ila ijulikane kwamba hakuna anayejua unabii wote, mengine BWANA hufunulia watu Wake yanapotokea ili wamtukuze na kujua hakika MUNGU anajishugulisha na maisha yao na NI KWELI tupu. Ukitaka kujua Zaidi soma Biblia umwombe MUNGU na fuata watu wanaosoma unabii huo kama wale wakina Ivor Myers na James Rafferty wa Salvation in symbols and signs (google).

Mwaka 1844 BK – Kristo aliingia Patakatifu pa Patakatifu mbinguni na kuanza hukumu ya upelelezi-Danieli 8:14.
Matukio haya yameandikwa na wanahistoria pia walioishi enzi hizo na hata wa

baadaye kama Josefas

*Haukuona kuwa ni kazi ngumu au mzigo ikiwa njia ingefunguka ili uweze kuwatunza watoto wako na kuwakinga kutokana na uovu ulioenea katika nyakati hizi za ulimwengu. Ulikuwa mzigo wa moyo wako kuwaona wao wakimgeukia Bwana. Uliomba mbele za MUNGU kwa ajili ya watoto wako kwa vilio vikali na machozi. Ulitamani sana uongofu wao. Wakati fulani moyo wako ulikata tamaa na kuzimia, na ukaogopa kwamba maombi yako yasingejibiwa; lakini ukawaweka tena wakfu watoto wako kwa MUNGU, na moyo wako wenye shauku uliwaweka upya juu ya madhabahu.

Kwa nini Kristo alikuja kwa Danieli wakati kama ule? Kulikuwa na ujumbe kwa ajili ya siku hizi za mwisho. Gabrieli akampasha habari Danieli, “Sasa nimekuja kukufahamisha mambo yatakayowapata watu wako [Israeli ya Kiroho] katika siku za mwisho; maana maono haya ni ya siku nyingi bado” (Dan.10:14). Kutokana na maombi ya bidii ya Danieli alionyeshwa mambo yatakayowapata watu wa Mungu siku za mwisho. Alipewa nuru ya kuyaelewa maneno ya Mungu ya kweli. Gabrieli alikuwa tayari kumfunulia zaidi juu ya Maandiko, akasema, “Lakini nitakuambia yaliyoandikwa katika maandiko ya kweli” (Dan. 10:21). Neno la Mungu ni Kweli; linatutakasa tukifanya lisemavyo (Yoh. 17:17; 7:17; 1 Petro 1:22-25; Yak. 2:22). Shetani siku hizi anawashawishi Wakristo wasisome Neno la Mungu ati kwa sababu wanaongozwa na Roho. Lakini kuna Roho Mtakatifu na “roho ya upotevu”, nguvu zote mbili zinawaongoza watu (1 Yoh. 4:1,6). Roho wa kweli kazi Yake ni kutufundisha Kweli, yaani, Neno la Mungu mpaka tulielewe vizuri kabisa (Yoh. 16:13-15; 14:21-26). Roho ya upotevu inatukataza kusoma wala kusikia Neno la Mungu. Yohana ametupa ruhusa kumpima Roho aliye ndani yetu, kujua ni wa aina gani, yaani, kama ni Roho wa Mungu kweli au ni roho ya upotevu. Mtu anayesema “Mimi naongozwa na Roho,” halafu anasema, “Sina haja ya kusoma, wala kulisikia neno la Mungu,” huyo haongozwi na Roho Mtakatifu, bali ile roho ya upotevu au “roho zidanganyazo,” yaani, “roho za mashetani” au “mapepo” (1 Tim. 4:1; Ufu. 16:13,14). Neno la Mungu linatuimarisha sana, hata pepo zivume namna gani hazitatuangusha (Mt. 7:24-27). Jikite juu ya Mwamba, yaani, Neno la Mungu au Kristo (Ufu. 19:13; Yoh.1:1-3). Neno na Kristo ni kitu kimoja tu. Huwezi kumpokea Kristo; na kulikataa Neno lake. Usirushwe-rushwe na kila upepo wa mafundisho; omba upewe mafungu ya Biblia kwa kila fundisho, utakuwa salama (Efe. 4:11-15). Jitahidi kusoma Biblia; itakuhekimisha hata upate wokovu wa kweli uliojengwa juu ya Neno, sio juu ya hisia na misisimko (2 Tim. 2:15; 2 Tim. 3:15-17)

---

Kutokana na unabii wa Daniel 8:14 kutakaswa kwa hekalu ni mwaka gani? Je Yesu alibatizwa mwaka gani kutokana na unabii huu wa Danieli 9? Je kuna binadamu anayejua unabii wote? Je tukisoma Unabii na tusipouelewa tufanyeje? Kwanini ni muhimu kujua unabii?

**SIKU YA 175**
**(Juni 23)**

# Maarifa Kuongezeka

**- Danieli 10-12**



Katika mwaka wa tatu wa Koreshi mfalme wa Uajemi, Danieli alikuwa akiomboleza kwa majuma matatu, akifunga mfungo ambao umejulikana kama 'mfungo wa Danieli" wa siku 21. Hakula vyakula vitamu, au vya fahari ambavyo vilikuwa vingi kwenye jumba la mfalme wa dunia yote siku zile. Kuna mifungo ya aina nyingi, huu ni mmojawapo. Baada ya kufika miaka12 waweza kujaribisha mfungo wa kula mara moja kwa siku, kama huna shida ya afya, mfano kisukari au vidonda vya tumbo.

Ikawa hizo siku 21 zilipotimia, Danieli aliinua macho yake na akaona Mtu amevikwa kitani, na viuno vimefungwa na mshipi wa dhahabu safi, mwili Wake kama zabarajadi safi na uso Wake kama umeme, na macho Yake kama taa za moto; mikono na miguu Yake kama shaba iliyosuguliwa sana, na sauti ya maneno yake kama umati wa watu. Danieli aliona haya peke yake, japo watu wengine walikuwapo. Ila watu hao walisikia tetemeko kuu, mpaka wakakimbia.

Danieli alipendwa sana, kwani aliambiwa mara kadhaa, "Ee Danieli, mtu upendwaye sana … Usiogope, kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele ya Mungu wako, maneno yako yalisikiwa, nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako. Lakini mkuu wa ufalme wa uajemi alinipinga siku 21, ndipo Mikaeli, mmoja wa wakuu wenu akaja kunisaidia. Danieli akaambiwa na malaika kwamba amekuja kumfahamisha mambo yatakayowapata watu wake siku za mwisho. Danieli aliona haya miaka zaidi ya 2500 iliyopita. Danieli aliposikia vile akawa bubu, na mmoja mfano wa wanadamu aligusa mdomo wake na akaweza

kunena tena, “Ee BWANA wangu kwa sababu ya haya maono huzuni zimenipata” maono haya yalikuwa mazito na ya kutisha.

Mwaka wa kwanza wa Dario, Mmedi Danieli akaona maono mengine, ya wafalme wa uajemi na mfalme wa kusini na kaskazini na yale watakayofanya mpaka mwisho wa wakati. Yaonekana Mfalme wa kaskazini na wa kusini wanaenda wakibadilika badilika, ila wote wapo upande wa adui Ibilisi. Iwe ni Urumi, Ufaransa, Babeli au Misri, falme zote zinazotajwa za kaskazini na kusini ni zile zinazoendeshwa kutokana na katiba za adui shetani. Waweza kuangalia watu ambao wamefanya utafiti Zaidi kuhusu hawa wafalme wa kusini na kaskasini kama vile (Ivor Myer, James Rafferty, Doug Batchelor, Stephen Bohr na wengine wengi). Vitabu vya Gems from the Book of Daniel and Gems from the book of Revelation na Patrick Jones, ni vitabu vizuri sana ambavyo vinalinganisha waandishi makini kadhaa wa unabii huo. Angalia program ya ‘Sign and Symbols’, nyingi zipo kwenye tovuti. Ila Daniel 2 na 7 na 8 zipo wazi Zaidi kuliko unabii mwingi wa kitabu hiki, na nchi zinatajwa na wala hutahitaji maelezo zaidi kama umesoma Historia ya dunia.

Kisha Danieli akaambiwa, “Mikaeli atasimama, Jemedari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati huo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakaonekana ameandikwa katika kitabu kile.” Mikaeli ni Yesu. Mungu anajua matendo yetu yote, anafungua vitabu si kwa ajili yake ila kwa sisi binadamu, wenye shauku ya kujua. Wengi watataka kujua “Kwa nini fulani hayupo hapa mbinguni? Au imewezekanaje mimi mbaya nikawa hapa? au kwa nini yule niliyefikiri ni mwovu sana yupo hapa?” Danieli anaeleza kuwa watu waliokufa watafufuka, ili wema wapate uzima wa milele, na waovu wapate aibu na kudharauliwa kwa milele.

Wale ambao wameishi maisha ya wema kwa kufuata Neno la Mungu “watang’aa kama mwangaza wa anga.” Na wale wanaosaidia wengine kutenda wema na haki “watangaa kama nyota milele na milele”. Danieli akaambiwa afunge Maneno ya kitabu na kuyaweka muhuri mpaka wakati wa mwisho. Ambao ndio sasa umefika maana aliambiwa wakati wa mwisho “wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka. Danieli aliona haya hata kabla ya baiskeli kutengenezwa. Ilikuwa wakati wa farasi tu!

Naamini umeshawahi kufikiri ni kwa nini wana wa Israeli hawakupanda mabasi au meli kwenda nchi ya ahadi! Au kwa nini Daudi hakumwua Goliathi na bunduki, au kwa nini Mamajusi hawakuchukua ndege kwenda kumwona Yesu wakati alipozaliwa. Haya yote hayakuwapo enzi zile. Huu sasa ndio wakati wa mwisho. Ndege inaenda km 1000 kwa sasa, Roketi inaenda mwezini km 27,000 kwa sasa. Leo dunia ni kama kijiji. Leo waweza kuwa Australia, kesho kutwa Uchina. Watu wanakimbia huko na kule kuwaambia watu habari njema. Simu zimekuja na kompyuta na hizi watu hutumia kuwasiliana, yaani, si lazima ubishe hodi kwa mtu. Na ukitaka kuongea na watu wengi, unatumia redio, zoom, simu na runinga. Na zaidi yote maarifa ya Mungu yameongezeka sana, kuliko nilivyokuwa mdogo, watoto wa umri mdogo wanajua Maandiko vyema sana kuliko zamani. Machapisho na kuenezwa kwa Neno






kunaendelea kila kukicha! Habari njema inahubiriwa kuwa ushuhuda, mwisho u karibu sana!

Mwaka wa 1884 ndipo gari lilivumbuliwa Ujerumani, Treni, cherehani na mengine ni vya miaka mia kadhaa iliyopita. Ndege ya kwanza kuruka kwa sekunde 8 na ndugu wawili wanaoitwa 'Wright Brothers' ilikuwa mwaka 1903. Mwanadamu alifika na kukanyaga mwezini mara ya kwanza mwaka 1969. Vifaa fulani vya umeme, mashine mbalimbali na hata plastiki vimekuja miaka ya 1960. Friji, mashine za kufua, X-ray, madawa ya penisilini, haya yote si mambo ya karne nyingi. Mambo karibu yote ya teknolojia tunayoyaona sasa yana miaka 150 tu hivi toka kuvumbuliwa katika uliwemwengu wetu wa historia ya miaka 6000. Angalia nyumbani kwako au shuleni, vifaa hivi, mababu zetu hawakuviona. Sisi tuna bahati kuviona na kuwa makini kujitayarisha kwa ufalme wa Mungu. Hatari ni kwamba ni maarifa yameongezeka na si hekima! Hekima ni kutumia maarifa tuliyonayo kwa ubora ili kuishi vyema na watu na MUNGU. Sulemani aliomba hekima, hakuomba maarifa au mali, Hebu nasi tuombe hekima ya kuwa na mahusiano mema na watu, na MUNGU pia.

Kutokana na unabii wa Danieli 9, siku za mwisho zinaanza baada ya zile ziku 2300 kwisha, yaani kwenye miaka ya 1800 hivi. Danieli aliona magari, pikipiki, kompyuta, baiskeli na mengine mengi, akashangaa ni mambo gani haya, alipata hofu na nguvu zikamwisha. Matukio mengine ya dalili za mwisho ni kama vile vita, matetemeko, uasi, dhiki, majanga mbalimbali na hata upendo wa watu kupoa. Mpendwa mtoto, omba, maana maneno ya Mungu ni rahisi, hata mtoto aliye mnyenyekevu anaweza kuelewa, maana Mungu Ndiye anayetufunulia unabii. Kitabu cha Ufunuo, kimefunua unabii wa Danieli katika mambo fulani.

Danieli akaambiwa ayafunge Maneno na kukitia muhuri kitabu mpaka wakati wa mwisho. "Wengi watajitakasa na kujifanya weupe na kusafika; bali wabaya watatenda mabaya." Ni wenye hekima tu ndiyo watakaoelewa kuwa mwisho umefika, au ni wakati wa kujitayarisha. Hekima ni kusoma Neno la Mungu, kulitafakari na kulitenda. Heri angojaye na kuzifikilia siku hizo. Na Danieli akaambiwa, "Enenda zako hata utakapokuwa mwisho ule; maana wewe utastarehe, nawe utasimama katika kura yako mwisho wa siku hizo." Bila shaka Danieli atakuwa mbinguni. Nafikiri hata wewe na mimi tunapenda kuwa pale, basi tupige mbio na kumtafuta Mungu usiku na mchana, ili tumjue na kufanya mapenzi Yake.

Kitabu cha Danieli kinahusu nyakati zetu hizi za mwisho. Kuelewa mambo yaliyo mbele yetu ni muhimu sana, maana ama tutapata uzima wa milele, ama mauti ya milele katika mkabala wetu na matukio hayo yanayokuja. Hivyo si suala dogo kujifunza unabii wa kitabu cha Danieli kwa wote wanaotaka uzima wa milele. Yesu akizungumza na wanafunzi Wake juu ya matukio ya siku za mwisho alisema, "Basi hapo mtakapoliona Chukizo la Uharibifu, lile lililonenwa na Danieli, limesimama mahali patakatifu (asomaye na afahamu)". Mathayo 24:15. Hatari kubwa i mbele yetu! Yesu anataka kila asomaye alifahamu Chukizo hilo la Uharibifu linalokuja ili atakapoliona akimbie kuokoa maisha yake (Mt. 24:16-22). Chukizo la Uharibifu limetajwa mahali patatu katika kitabu cha Danieli (Dan. 9:26,27; 11:31; 12:11). Lina majina mengi katika kitabu cha Danieli na cha Ufunuo.
----- Pembe Ndogo, Mnyama, na kadhalika. Utashangaa kujua kwamba "mnyama" katika lugha ya taaluma ya unabii sio tusi wala kashfa kama wengi wanavyodhani. Maana yake ni "mfalme au ufalme" (Dan.7:17). Biblia inajitafsiri yenyewe!

Watoto wa Mungu wamechoka na dunia hii wanataka kwenda kupumzika mbinguni kwa miaka 1000, na Yesu anasema. " Tazama, Naja upesi, na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo" (Ufu. 22:11). Je! u tayari kumlaki Bwana? Je! utasimama imara hata kama mbingu zikianguka, na kuiinua juu Bendera ya Imanueli [Kristo] iliyoandikwa "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao Amri [Kumi] za Mungu, na Imani ya Yesu" (Ufu. 14:12). Hivi karibuni dunia hii itabaki tupu, ndugu yangu. Kuanzia leo chagua kuingia Paradiso pamoja na Kristo (Luka 23:42,43; 2 Kor. 6:2). Huenda usisikie mwito mwingine kama huu. Amua leo!

*MUNGU hatakataa kusikia maombi ya dhati na bidii ya wazazi, ambayo yanaungwa mkono na bidii ya kudumu, ili watoto wao wapate baraka kutoka Kwake, na kuwa wafanyakazi waaminifu katika kazi Yake. Wazazi wanapofanya wajibu wao kwa njia iliyowekwa na MUNGU, wanaweza kuwa na uhakika kwamba maombi yao ya msaada Wake katika kazi yao ya nyumbani yatakubaliwa.

---

Kuna tofauti gani kati ya hekima na maarifa? Mfungo wa Danieli una maana gani? Wengi watajitakasa, ila wabaya watatenda mabaya ina maana gani? Ni vitu gani vimevumbuliwa miaka 150 hivi iliyopita, viorodheshe! Siku 1260 ni sawasawa na miaka mingapi ya unabii? Ni akina nani watang'aa kama mwangaza wa anga? Je, wewe unataka kung'aa?

**SIKU YA 176**
**(Juni 24)**

# Upendo wa Mungu kwa Watu Wake

**- Hosea**



Hiki ndicho kitabu cha kwanza cha manabii wadogo, yaani, wenye vitabu vifupi. Aliandika kama mwaka 755 KK kwa Israeli, na si Yuda. Lengo lake kubwa ni kuonesha jinsi Israeli ilivyomwacha Mungu, sawa na mwanamke aliyemwacha mume wake na kuchukuliwa na wanaume wengine, lakini bado Mungu alidumu kuwapenda. Hosea alikuwa na ujumbe kwa ufalme wa kaskazini wa Israeli, watu hawa waliwaonea watumwa na kuabudu miungu mingine. Israeli ndiyo ilianza uasi mkubwa kabla ya dada yake Yuda. Neno la BWANA lilimjia Hosea mwana wa Beeri siku za Uzia, Yothamu, Hezekia, Ahazi, wafalme wa Yuda na Yeroboamu mfalme wa Israeli.

Hosea anaanza kitabu chake na maagizo aliyopewa na Mungu kwamba aende akamchukue mwanamke asiye mwaminifu, anayeenda na wanaume wengine, yaani, mzinzi. Ndoa ni agano kati ya mume na mke, na ni mfano wa uhusiano wa Mungu na watu wake. Hosea akamwoa mwanamke aitwaye Gomeri, na kutoa mahari. Mke akapata mtoto, Mungu akamwambia amwite Yezreeli, ikiwa ina maana, "Mungu ataipa adhabu nchi ya Israeli" wakati Yehu anatawala.

Kisha wakapata mtoto wa kike, naye akamwita Loruhama, yaani, asiyependwa au 'atakayekosa huruma.' Israeli ilikuwa imetanga mbali na maagizo ya BWANA japo Yuda bado walikuwa na msimamo. Kisha Gomeri akapata tena mtoto wa kiume akaitwa jina lake Loami, maana yake Israeli "si watu Wangu."

Kuachwa kunazungumzwa hapa kwamba Hosea atamwacha mke huyu mwovu, kama ambavyo Mungu ataiacha Israeli, kwa ajili ya kukosa uaminifu na kwenda kwa miungu mingine. Anaeleza kwamba kuna siku atafanya upya agano lake na kuwachukua Israeli tena. Basi Mungu anamwambia Hosea aende akamtafute tena Gomeri, aliyejiuza kuwa mtumwa, atoe tena pesa ili kumtoa katika kongwa hilo, amchukue nyumbani na kuwa mke wake tena. Mungu akasema Waisraeli watakaa siku nyingi bila mfalme, wala kuwa na shuguli za ukuhani, kisha watarudi wamtafute BWANA Mungu wao kwa kicho siku za mwisho. Nasi pia leo tunaitwa turudi na kumtafuta BWANA.

Hosea anakuwa kielezo kupitia ndoa yake chungu au ngumu, kueleza kwamba Israeli imekosa uaminifu kwa Mungu. Hakuna mwanamume anayetaka mke wake achukuliwe na mwanamume mwingine. Mungu Naye hataki tuchukuliwe na miungu mingine kwani ni baba yetu na Ndiye aliyetuumba. Mungu anawahimiza waombe msamaha na kuacha uovu wao. Mungu anasema "watu Wake wanaangamizwa kwa kukosa maarifa." Hata leo, wengi waangamia kwa kukosa kujua Neno la BWANA, aidha kwa kutolisoma au kwa kutolitenda. Kukataa maarifa ya Neno la Mungu, ni kukataa sheria za Mungu. Mungu anasema Waisraeli wangekula ila wasingeshiba, walitenda kwa hila, kabila la Efraimu linazungumziwa kwa kufuata uovu kirahisi. Walikuwa kama mkate ulioiva upande mmoja, wageni walikula nguvu zake naye hakuwa na habari. Efraimu alikuwa kama njiwa mpumbavu asiye na ufahamu, akimwita Misri kwenda Ashuru, akimkimbia Mungu na angepata uharibifu. Watu walijenga ndama Samaria na kuiabudu, walipanda upepo na wangevuna tufani, kwa kutoa kafara kwa miungu mingine na kuiabudu.

Kitabu hichi kinatueleza upendo mkuu wa Mungu. Tangu uumbaji, binadamu ameonesha kutokuwa na shukurani na kuzama katika uovu. Hata hivyo, Mungu amedhihirisha upendo Wake kwa wanadamu. Je, mtoto anayepewa upendo wote, rehema na neema, anaweza kumkosea babaye adabu? Ndiyo, kama ambavyo tumefanya, tunapofikiri hili, tujione sisi kama Waisraeli na kumrudia BWANA. "Njooni tumrudie BWANA, maana Yeye amerarua Naye atatatuponya, amepiga Naye atafunga jeraha zetu…baada ya siku mbili atatufufua na siku ya tatu atatuinua nasi tutaishi milele mbele Zake." Mungu anataka tutende fadhili kwa watu na si sadaka, na kumjua Mungu ni bora kuliko kutoa sadaka.

Efraimu analinganishwa na ndama anayependa kupura nafaka ili ale. Anafikiria kuhusu yeye na anasa zake tu. Mungu kama mzazi anamwita Efraimu kutoka Misri kwenye utumwa. Mungu anatufundisha kama mzazi. Upendo wa Mungu unatuponya na kutuhuisha. Mungu hatulipizi kisasi, bali anatuadibisha kama watoto Wake.

Tukiangalia kioo, tunajiona wenyewe na si mwingine. Tukumbuke wema na upendo wa Mungu, na kumcha Yeye tu. Kitabu cha Hosea kinaonesha jinsi ambavyo tumekosa wote na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Lakini kama tukimrudia Yeye kwa kutubu na kuungama, Mungu atatuponya kurudi nyuma kwetu Yeye ataendelea kutuonesha upendo Wake usio na kikomo. Njia za BWANA zimenyoka Naye ametuonesha mahali pa kukanyaga, hebu tuombe hekima ili tuenende katika njia Yake ya haki.

Ukiwa unajiuliza upendo wa Mungu kwako ni kiasi gani, rudia kitabu cha Hosea, uone upendo Wake. Je, Gomeri alistahili upendo wa mume wake? La! Je sisi tunastahili upendo wa Mungu? La! Lakini kwa neema na huruma Zake, anataka turudi Kwake kwani, Mungu Ndiye BWANA na Mwokozi; hakuna mwingine mbinguni wala duniani isipokuwa YEYE. Kwa masikitiko alisema, "Niwezeje kukuacha Efraimu?" Bwana anataka kutuokoa na hataki yeyote apotee bali wote tufikilie toba.
Leo tujiulize. Je tuna miungu mingine? Iwe ni matumbo, elimu, uzuri, maoni, mali, uraibu na mengineyo. Ikiwa Israeli wangeweka uhusiano mzuri na Mungu, mbingu na dunia zingeitikia na ardhi ingewapa chakula (2:22). Tuna Mungu Mwenye rehema kama nini!

Wanasayansi wa neva wanazungumza kuhusu dhana inayojulikana kama "neuroplasticity," ambayo ni mpya kabisa, hii ni uwezo wa ubongo kuanzisha njia mpya za neva na hivyo kujielekeza upya. Watu ambao wanapambana na tabia za uraibu wanahimizwa kuepuka, na wakati mwingine kukata kabisa, watu, mahali na vitu vinavyoendekeza uraibu wao. Katika njia hii ya kupona, ubongo unaweza kujielekeza upya na kuruhusu uundaji wa mifumo mipya ya tabia. Kama vile Mungu alivyofanya na Israeli, anatutambulisha katika kutunyima mambo ambayo ni kikwazo cha kuendelea kukua ndani Yake. Ingawa mchakato huo ni mchungu, mwanzoni unaonekana kama jambo la starehe, ila mambo ya kiroho yanaondolewa. Uzuri ni kuwa hatimaye mambo ya Israeli yalikuwa mazuri. Mwishoni mwa mchakato wa mashida, Israeli walirudi na kumtafuta Mungu (3:5). Je, ni kwa njia zipi Mungu anatoa vikwazo katika maisha yako na yangu nami napawa kumshukuru kwa hilo? Hebu asiseme haya kwetu "Efraimu ameshikamana na sanamu zake, mwacheni" (4:17).

Mazoezi ya uasi ya kuabudu sanamu hatimaye hudhoofisha hisi. Mtu huyo anakuwa kiziwi kwa sauti ya kusihi ya Roho Mtakatifu; wanakuwa vipofu wanapotembea kwenye njia ya maangamizi na maonyo ya busara yanapuuzwa. Hili ndilo ambalo baadaye lingemfanya Yesu aseme kwa Mafarisayo kwamba wao pia waachwe peke yao, kwa kuwa walikuwa wamekwenda mbali sana (Mathayo 15:14).

Je, tunazuiaje hili lisitutokee? Inaanza kwa kumruhusu Yesu achunguze mioyo yetu na kutukomboa kutoka katika kujidanganya kwa dhambi. Ataonyesha njia ambazo tunaweza kuwa tunajiunga na sanamu ambazo zinaua usikivu wa Roho Mtakatifu. Tunashirikiana Naye kuwaondoa. Je, kwa kujua au kutojua umejiunga na sanamu zozote?

Mungu alitoa maagizo mengi yaliyoandikwa ili kuwaongoza, lakini kwao mafundisho ya Mungu yalikuwa ya ajabu (8:12). Walipenda matoleo yao ya dhabihu kwa sababu walipenda kula nyama na kula walichotaka. Mungu alitamani toba yao na utii kwa mafundisho yake badala ya wingi wa dhabihu (8:13).

Kwa nini Israeli na Yuda walishindwa kumtambua Mungu kuwa Muumba na Mtegemezi wao? Je, tunamkumbuka Mungu kama Muumba, Mwokozi, na Mkombozi wetu kila siku? Je, matendo yetu yanapingana na ukiri wa imani yetu?

*Kesha kila wakati ili kukata mkondo na kurudisha nyuma uzito wa uovu ambao Shetani anausukuma juu ya watoto wako. Watoto hawawezi kufanya hiliwenyewe. Wazazi wanaweza kufanya mengi. Kwa ombi la dhati na bidii na imani iliyo hai, ushindi mkubwa utapatikana.

---

Lengo la kitabu cha Hosea ni nini? Mungu anaoneshaje upendo Wake kwa Israeli? Je, ni kwa namna gani leo tu kama mke wa Hosea? Kwa nini Mungu ni Mwenye huruma? Yezreeli ina maana gani? Je, Mungu anaoneshaje upendo Wake kwako leo? Nabii mdogo ina maana gani?

**SIKU YA** 177
**(Juni 25)**

# Ujumbe wa Yoel-Nitakuachaje, Nitakuokoaje, Eh Israeli?

Yoeli ina maana Yehova ni Mungu. Yoeli aliandika kitabu chake miaka ya 835 KK, kwa watu wa Yuda. Watu wa Yuda walikuwa na mafanikio sana, na ndipo wakajisahau kwa sherehe na kunywa hata kulewa. Hakuna ubaya kufurahia baraka za Mungu, lakini zisitufanye tuishi kwa ubatili. Ujumbe wa Yoeli unatolewa kwa Yuda ili wapate kumrudia BWANA.

Waliambiwa, "Yaliyosazwa na tunutu yameliwa na nzige, na yaliyosazwa na nzige yameliwa na parare, na yaliyosazwa na parare yameliwa na madumadu." Nzige walikula mizabibu, nafaka, na miti yote, hata mifugo ikakosa malisho. Furaha na vicheko vikaisha, na mbegu zikaoza ardhini na nchi ikabaki ukiwa. Makuhani hawakuwa na sadaka ya kutoa. Njaa na shida zilikuwa vilienea. Walionywa kuwa "Siku ya BWANA inakaribia, nayo itakuja kama uangamivu kutoka Kwake Mwenyezi." Yoeli anafananisha nzige na majeshi ambayo yangekuja kuiadhibu Yuda kwa sababu ya dhambi zake. Kutakuwa na giza na weusi, mfano wake hautakuwako kamwe, naye ni nani awezaye kustahimili? Nyuso za watu zitageuka kwa hofu, na watapiga mbio na kuingia kupitia madirishani kama aingiavyo mwizi, nchi itatetemeka, jua na mwezi litatiwa giza. Furaha yao yote itaondolewa.Yoeli anawaambia wakuu na taifa lote, watangaze siku ya maombi ya taifa, wachunguze



njia zao na kujirekebisha. Maagizo ya Yoeli na ahadi ni zetu pia leo.



BWANA anatuagiza akisema, "Nirudieni Mimi, kwa mioyo yenu yote kwa kufunga na kwa kulia, na kwa kuomboleza; rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu, mkamrudie BWANA, Mungu wenu; kwa maana Yeye Ndiye Mwenye neema, amejaa huruma; si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa rehema, Naye hughairi mabaya." Baadaye anawaambia watu wa Yuda kuwa wafurahi na wasiogope, washangilie kwa kuwa BWANA atatenda matendo makuu na mazao yatatoa tena matunda, na wanyama watakuwa na malisho.

Yoeli anawaambia kuwa BWANA atatoa mvua ya vuli na ya masika, kama kwanza. Ngano ingejaa tena, na divai na mafuta yatafurika. Na ile miaka ambayo nzige, parare, madumadu na tunutu wamekula, BWANA atarudisha. Watakula chakula tele na kulihimidi Jina la BWANA aliyewatendea mambo ya ajabu; na watu Wake wasingetahayari kamwe.

BWANA anasema kuwa siku za mwisho atamimina roho Wake juu ya wote wenye mwili, na wana wa kiume na wake watatabiri, wazee wataota ndoto, na vijana wataona maono. BWANA ameahidi kuwa "Kila mtu anayeliita Jina la BWANA ataokolewa." Siku za mitume, wakati wa Pentekoste, wanafunzi walipokea ujazo wa Roho Mtakatifu. Mtume Petro alinukuu Yoeli na kusema, "Lakini jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli, "Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono, na wazee wenu wataota ndoto … Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi Wangu wanaume na wanawake Roho Yangu watatabiri."

Anamalizia kwamba siku za mwisho makutano makubwa watakutanika katika bonde la kukata maneno. Jua na mwezi vitatiwa giza, na nyota zitaacha kutoa mwanga wake, nchi itatetemeka, lakini BWANA atakuwa kimbilio la watu Wake. Tumaini letu lisiwe kwenye vitu vyetu au sisi wenyewe, bali kwa BWANA, hivyo tumtafute BWANA maadamu anapatikana. Ni wakati wa kuwaambia wengine habari njema za ufalme wa Mungu na "kutia mundu maana mavuno yameiva," na ni mengi ila watenda kazi ni wachache." Mwito ni kuungama na kumrudia BWANA maana tunaishi siku ambazo unabii huu unatimia machoni petu. Wale wanaoungama kwa toba ya kweli na kutembea katika ile Kweli Yake, hawataaibishwa kamwe.
Hebu tumrudie Mungu kwa moyo wetu wote, kwa kufunga na kulia na kuomboleza, na turarue mioyo yetu.

*Kufanya kazi yake inavyopaswa kufanywa kunahitaji talanta na ustadi na uvumilivu wenye umakini mkubwa. Inahitaji kutojiamini nafsi na kuomba kwa bidii.

Hebu kila mama na ajitahidi kwa bidii katika kutimiza wajibu wake. Hebu awalete watoto wake wadogo kwa Yesu kwa mikono ya imani, akimwambia Yeye hitaji lake kubwa, na kuomba hekima na neema.

---

Rarueni mioyo yenu na si mavazi yenu ina maana gani? Ahadi ya mvua ikoje? Siku za mwisho wazee, vijana na wanawali watapata nini? Siku ya Pentekoste wanafunzi walipata kitu gani? Siku ya BWANA ina maana gani?

**SIKU YA 178**
**(Juni 26)**

# Nabii Amosi



Nabii Amosi alitoka katika mji mdogo ulioitwa Tekoa, na alikuwa mchungaji wa mifugo na mkulima wa mikuyu. Nyumbani kwake palikuwa ni Yuda, ufalme wa Kusini, lakini alitumwa kupeleka ujumbe ufalme wa Kaskazini wa Israeli. Alikuwa nabii wakati wa mfalme Uzia wa Yuda na Yeroboamu wa Israeli. Mungu alitaka watu wake wawe na hukumu za haki na huruma ili "hukumu itelemke kama maji na haki kama maji makuu." Watu walikuwa na utajiri katika nchi, na nyumba kubwa na wengine nyumba za wakati wa joto na wakati wa baridi. BWANA alisema watu wanawaonea maskini na wenye mahitaji. Hata leo, lazima watu wawe waangalifu kujali na kuhurumia yatima, wajane, wageni, wenye shida na maskini. Tusipunguze thamani ya watu machoni petu, kwani Mungu anawathamini wote, awe ni maskini, mjane, yatima, mgeni, au mtu asiye kabila letu. Tumtafute BWANA tukaishi. Israeli ilipaswa iwe ni hubiri kwa watu wa mataifa, maana Mungu aliwabariki mno. BWANA akawaambia kuwa atawahukumu, na kwa sababu hiyo, "wajiweke tayari kuonana na Mungu wao."

Fikiria ikiwa wanafunzi wa Kristo wangeuliza swali, "Ni nini kinachomkasirisha Yesu?" Jibu lao lingeweza kuwa, "Udhalimu katika Nyumba ya Bwana." Mahusiano na vitu vya Mungu vilifanya dhamiri zao zisiwe na maadili hivi kwamba hawakuweza kutambua tishio lililokuwa dhidi yao. Wacha sisi tupeleleze kwa kina kumpendeza Kristo leo katika mawazo na matendo yetu na kufanya hivyo.

BWANA anauliza Waisraeli, Je! watu wawili wanaweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana? Je, simba atanguruma mwituni asipokuwa na mawindo, je, ndege ataanguka mtegoni juu ya nchi mahali bila chochote, au tarumbeta itapigwa watu wasiogope? Mungu anaahidi kuwa hakika hatafanya jambo lolote kwa kushtukiza, bila kuwafunulia watumishi Wake manabii siri Yake. Hata leo Mungu ameendelea kujifunua kwetu, hivyo hatuna sababu ya kutembea kama kipofu au gizani. Amosi hakutaka kuwa kama manabii waliotabiri ili wapate mali. Bali alisema kama Mungu alivyomfunulia. Ukweli mara nyingine unauma na kufanya watu wamchukie na kumtweza nabii.

Kitabu hiki kina lengo ya kutangaza hukumu ya Mungu kwa ufalme wa kaskazini, wa Israeli na pia kwa mataifa kadhaa. Yuda ilikuwa kusini. Watu wanaambiwa watubu na kuacha miungu migeni na dhambi ya kujiona kuwa wao ni watakatifu. Walikuwa watu wa dini lakini walikuwa wanafiki - wakila rushwa, na kuwageuza wahitaji langoni wasipate haki yao. Amosi anasema mataifa ya jirani pia kama Dameski, Gaza, Edomu na Tiro wataangamizwa kwani "SIKU ya BWANA" inakuja. Wakaambiwa, "tafuteni mema wala si mabaya, mpate kuishi; hivyo BWANA Mungu wa majeshi, atakuwa pamoja nanyi kama msemavyo." BWANA akawaambia kuwa, "Siku hiyo nitainua tena maskani ya Daudi, iliyoanguka, na kuziba mahali palipobomoka; Nami nitayainua magofu yake na kujenga kama siku za kale. Siku hizo Mungu atapanda watu katika Yerusalemu mpya, wala watu hawatang'olewa tena watoke katika nchi yao niliyowapa asema BWANA Mungu wako."

Ujumbe ufuatao ni wa muhimu sana kwetu leo, BWANA anasema, "Nami nitazigeuza sikukuu zenu kuwa maombolezo, na nyimbo zenu zote kuwa vilio; nami nitatia nguo za magunia katika viuno vyote, na upaa katika kila kichwa; Nami nitayafanya haya kuwa kama maombolezo kwa ajili ya mwana wa pekee, na mwisho wake kama siku ya uchungu. Angalia, siku zinakuja, asema Bwana MUNGU, ambazo nitaleta njaa katika nchi; si njaa ya kukosa chakula, wala kiu ya kukosa maji, bali ya kukosa kuyasikia Maneno ya Bwana. Nao watatanga-tanga toka bahari hata bahari; na toka upande wa kaskazi hata upande wa mashariki; watapiga mbio, wakienda huko na huko, kulitafuta neno la Bwana, wasilione. Siku hiyo wanawali wazuri na wavulana watazimia kwa kiu"

*Juhudi zenye bidii na zenye maumivu, maombi na imani, vikiunganishwa na mfano sahihi, havitakosa matunda. Walete watoto wako kwa MUNGU kwa imani, na utafute kushawishi akili zao kupata hisia ya wajibu wao kwa Baba yao wa mbinguni.

---

Kazi ya Amosi kabla ya kuitwa kuwa nabii ilikuwa nini? Amosi anatoa ujumbe wake kwa watu gani? Je, watu wawili waweza kutembea pamoja isipokuwa wamepata? Je, hili linatuhusuje sisi na marafiki zetu? Watu walikuwa wanafanya ubaya gani kwa wengine? Onyo la mwisho ni lipi?.

# Ujumbe wa Mika

Kitabu hiki kiliandikwa na nabii Mika, Mmorashti, miaka ya 735KK, wakati mfalme Yothamu, Ahazi na Hezekia wanatawala. Maono haya yalikuwa kwa Samaria na Yerusalemu, yalikuwa na hukumu na matumaini. Amosi na Hosea walikuwa wameshughulikia hili pia. Mara zingine hukumu ni kitu cha matumaini kwani watu hubadilisha njia zao mbovu na kuokolewa. Ni nani aliye kama Mungu, mwenye kusamehe uovu na kuliachia kosa la watu wa urithi wake waliosalia? Hashiki hasira yake milele, kwa maana hufurahia rehema." BWANA hurejea na kutuhurumia, anakanyaga maovu yetu na kuzitupa dhambi zetu zote katika vilindi vya bahari.



Nabii Mika anatoa onyo akisema, "Ole wao wakusudiao mambo maovu, na kutenda mabaya vitandani mwao! Kunapopambazuka asubuhi huyafanya, kwa sababu ya katika uwezo wa mikono yao. Nao hutamani mashamba, na kuyashika; na nyumba pia, nao huzichukua; nao humwonea mtu na nyumba yake, naam, mtu na urithi wake. Basi Bwana asema hivi, Angalia, nakusudia jambo baya juu ya jamaa hii, ambalo hamtazitoa shingo zenu, wala hamtakwenda kwa kiburi; kwa maana ni wakati mbaya." Mungu anatoa ilani watu waondoke maana hapa sipo mahali pa raha au mapumziko yao. Kwa sababu ya uchafu wataangamizwa, naam, kwa maangamizo mazito sana.

Manabii na makuhani walikuwa wanatoa unabii wa uongo kwa faida yao wenyewe. BWANA akawaambia, "mnakula nyama ya watu Wangu, na kuwachuna ngozi zao, na kuivunja mifupa yao; naam, kuwakata vipande vipande kama kwa kutiwa chunguni, na kama nyama sufuriani. Ndipo watakapomwomba Bwana, asiwaitikie; naam, atawaficha uso Wake wakati huo, kwa kadiri walivyotenda mabaya kwa matendo yao. Bwana asema hivi katika habari za manabii wanaowakosesha watu Wangu; hao waumao kwa meno yao, na kulia, Amani; na mtu awaye yote asiyetia kitu vinywani mwao, wao humwandalia vita. Kwa hiyo itakuwa usiku kwenu, msipate kuona maono; tena itakuwa giza kwenu, msiweze kubashiri; nalo jua litawachwea manabii, nao mchana utakuwa mweusi juu yao. Na hao waonaji watatahayarika, na wenye kubashiri watafadhaika; naam, hao wote watajifunika midomo yao; kwa maana; hapana jawabu la Mungu."

Mika anatoa unabii wa Masihi kwa wengi waliopoteza maana ya maisha. Mika 5:2 Yasema "Bali wewe Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu wa Yuda; kutoka kwako wewe atatokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo Yake, yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele… Naye atasimama na kulisha kundi Lake kwa nguvu za BWANA kwa enzi ya Jina la BWANA, Mungu Wake; nao watakaa; maana sasa atakuwa mkuu hata miisho ya dunia."

Mika aliishi wakati wa viongozi na matajiri waliojaa jeuri, uongo na vipimo vilivyopunguka; watu waliweka mifukoni mwao mawe ya kupimia ya udanganyifu. Walifikiri kuwa watapata baraka kwa vile ni Waisraeli, wakisahahu laana za Kumbukumbu la Torati 28. Yeye ajidhaniaye amesimama aangalie asianguke. Watu wamchao Mungu walitoweka, wala hapana aliyekuwa adili, wote waliotea kumwaga damu na kuwinda ndugu zao, mikono ilishika mabaya ili wayatende kwa bidii, makadhi walikula rushwa, na kunena madhara. Mtu aliye mwema hawakumpenda, akaonekana kama miiba. Hata mtu na mke wake walikuwa wakifanyiana ubaya. Mwana alimwaibisha babaye, na binti aliondoka ashindane na mamaye, na mwanamke aliyeolewa kushindana na mama mkwe wake. Maadili yalikuwa yameshuka katika jamii. Unaonaje maadili katika jamii ya sasa?

Mika anatoa ufumbuzi wa kile BWANA anachohitaji kwetu, cha muhimu kupita vyote. Watu walisema wamechoshwa na mateto ya Mungu. BWANA akawaambia yale aliyowafanyia toka Misri, walikuwa wamesahau alipowatoa na kuwafanyia wema? Anauliza amkaribie Mungu na kitu gani, Je, amkaribie na sadaka za kuteketezwa, ndama za umri wa mwaka mmoja? "Je! BWANA atapendezwa na elfu za kondoo waume, au na elfu kumi za mito ya mafuta? Je! nimtolee mzaliwa wangu wa kwanza kwa kosa langu, mzao wa mwili wangu kwa dhambi ya roho yangu?" Anajibu hili swali, yaani lile Mungu analohitaji kwetu hata leo, anasema, "Ee mwanadamu, YEYE amekuonyesha yaliyo mema, na BWANA anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako."

Adhabu ya udhalimu au kukosa rehema ni pigo liumizalo sana, "Utakula, lakini hutashiba; na fedheha yako itakuwa kati yako; nawe utahama, lakini hutachukua kitu salama; na hicho utakachochukua nitakitoa kwa upanga. Utapanda, lakini

hutavuna; utazikanyaga zeituni, lakini hutajipaka mafuta; na hizo zabibu, lakini hutakunywa divai."

Mungu anatoa maonyo kwetu leo kama kwa nabii Mika, ili tusipate adhabu ya ghadhabu Yake. Ni hakika hukumu yaja atashuka na kupakanyaga mahali pa dunia palipoinuka, na hiyo milima itayeyuka chini yake, nayo mabonde yatapasuliwa, na kuyeyuka kama vile nta iliyo mbele ya mto, kama maji yaliyomwagika tena kutelemkia chini.

Ufumbuzi ni kumpokea Yeye, Mungu wetu. Dhambi inatuangamiza, na Mungu anaahidi kwamba tutakuwa kamili katika Yeye kama tukimtii. Ni nani aliye Mungu kama Yeye, Mwenye kusamehe uovu? Mika anajipatia matumaini kwamba, "Lakini mimi nitamtazamia BWANA, nitamngojea Mungu wa wokovu wangu; Mungu wangu atanisikia. Usifurahi adui juu yangu, Ee adui yangu; niangukapo nitasimama tena, nikaapo gizani, BWANA atakuwa nuru kwangu." BWANA anatupenda kuliko tunavyojipenda, na wale tunaowapenda, Yeye anawapenda zaidi yetu.

*Akina baba na akina mama, je, hamtashikilia kazi yenu kwa nguvu, uvumilivu, na upendo? Panda mbegu ya thamani kila siku, kwa maombi ya dhati ili MUNGU aimwagilie kwa umande wa neema, na kukupa mavuno mengi sana. Mwana wa MUNGU alikufa ili kukomboa jamii ya bindamu yenye dhambi na iliyoasi. Je, tujiepushe na taabu, kujitoa kujitoa mhanga au dhabihu yoyote ili kuokoa watoto wetu wapendwa?

---

Mungu anahitaji tufanye mambo gani matatu? Bethlehemu ya Yuda kwa nini si mdogo? Tumaini la Mika ni lipi?

**SIKU YA 180**
**(Juni 28)**

# Yona - Nabii Aliyemezwa na Samaki



Baada ya kifo cha Elisha, Yoashi mfalme wa Israeli akaenda vitani na Ben Hadadi II, mfalme wa Ashuru na kumshinda mara tatu kama Nabii Elisha alivyotabiri. Waashuru walikuwa wanyanganyi, wakatili na wadhalimu. Katika kipindi hicho ndipo akainuka nabii aitwaye Yona, akihubiria Waisraeli. Na Neno la BWANA likamjia Yona mwana wa Amitai, aondoke kwenda Ninawi, mji ule mkubwa, akapige kelele juu yake, maana uovu wao ulikuwa umepanda juu mbele za Mungu. Lakini Yona hakupenda kwenda, akaondoka akimbie kwenda Tarshishi apate kuukimbia uso wa BWANA; kwa kuwa hawa Waashuru walikuwa maadui wa nchi yake Israeli. Alitamani kulipiza kisasi, akiacha watu wa Ninawi wafe katika dhambi zao bila ya kumrudia BWANA. Tarshishi ni mojawapo wa sehemu zilizokuwa zinajulikana kama 'ukingo' au mwisho wa dunia, ukifika huko waliamini dunia si tufe, na hivyo ungetumbukia kwenye shimo! Akaenda Yafa bandarini, akakata tiketi na kupanda merikebu ya kwenda Tarshishi ili amkimbie BWANA. Lakini BWANA alituma tufani kubwa baharini, na hata merikebu ikawa karibu kuvunjika. Mabaharia wakaogopa sana, na kama kawaida, wengi humlilia Mungu wakiwa na shida, ila mambo yakiwa shwari husahau. Watu hawa wa merikebuni wakaanza kila mtu kumwomba mungu wake. Wakajaribu kupunguza shehena merikebuni ili kupunguza uzito, lakini haikusaidia. Yona alikuwa ameshuka hata pande ya chini ya merikebu na akapata usingizi wa fofofo. Basi nahodha akamwendea na kumwuliza, "Una nini, Ewe ulalaye

usingizi? Amka, ukamwombe Mungu wako; labda Mungu huyo atatukumbuka, tusipotee." Wakasemezana wapige kura, na itakayemwangukia, basi ni huyo ndiye ameleta janga hili. Walipopiga kura, kura ikamwangukia Yona. Wakamhoji maswali mfululizo, "wewe ambaye mabaya haya yametupata kwa sababu yako; kazi yako ni kazi gani? Nawe umetoka wapi? Nchi yako ni nchi ipi? Nawe u mtu wa kabila gani? Yona, akajibu "mimi ni Mwebrania, nami namcha BWANA, Mungu wa mbinguni, aliyeziumba bahari na nchi kavu." Hii ndiyo tofauti kubwa kati ya Mungu wa Kweli na miungu isiyo ya Kweli. Wale watu wakaogopa mno, wakasema, "jambo gani hili ulilolitenda!" Watu hawa walijua fika kwamba huyu ni mkimbizi, amekimbia ajiepushe na BWANA au jukumu ambalo BWANA amempa, kwani mwenyewe alikuwa amekiri.

Wakamwuliza wamfanye nini, ili bahari itulie? Akasema wamtupe baharini, na bahari itakuwa shwari, "kwa maana najua ya kuwa ni kwa ajili yangu tufani hii imewapata." Lakini wale watu hawakutaka kumtupa, wakajaribu wavute makasia ili wafike pwani, lakini bahari ikazi kuwachafukia sana. Basi watu hawa ambao walikuwa hawamwabudu Mungu wa kweli, walianza kwa mara ya kwanza kumlilia BWANA na kusema, "Twakuomba, Ee BWANA, tusiangamie kwa ajili ya uhai wa mtu huyu, wala usitupatilize kwa ajili ya damu isiyo na hatia, kwa maana wewe BWANA umefanya kama ulivyopenda." Walikuwa hawana uchaguzi isipokuwa kumtupa Yona majini, na wakafanya hivyo. Mara tu walipomtupa Yona, bahari ilitulia kabisa.

Ndipo wale watu wakamwogopa BWANA mno, wakamtolea sadaka na kuweka nadhiri. BWANA akaweka tayari samaki mkubwa ili ammeze Yona, naye Yona akawa ndani ya samaki kwa siku tatu, mchana na usiku. Wakati akiwajibu wale waliomtaka aoneshe ishara, Bwana Yesu alisema kuwa kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la samaki, ndiyo mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

*Baada ya kufanya wajibu wako kwa uaminifu kwa watoto wako, basi wabebe na uwapeleke kwa MUNGU na umwombe akusaidie. Mwambie kwamba umetimiza sehemu yako ya Sala ya Maombezi, kisha kwa imani umwombe MUNGU afanye sehemu Yake, ambayo wewe hauwezi kuifanya. Malaika Huweka katika kumbukumbu Kila Ombi la Dhati—Tunapaswa kumfahamu MUNGU sasa kwa kuthibitisha ahadi Zake. Malaika huweka katika rekodi kila ombi ambalo ni la dhati na lenye bidii. Afadhali tutupilie mbali kuuridhisha ubinafsi kuliko kupuuza ushirika na MUNGU. Umaskini mkubwa zaidi, kujikana zaidi pamoja na kibali Chake, ni bora kuliko utajiri, heshima, urahisi wa maisha, na urafiki bila kibali Chake. Ni lazima tuwe na muda wa kuomba.

---

Somo hili linatufundishaje kuwa BWANA anajua mawazo yetu yote? Kwa nini Yona alikimbia? Kwa nini mabaharia waliogopa na kumtukuza Mungu? Je, leo wewe unawakimbia nani? Yona alikuwa ndani ya samaki siku ngapi?

**SIKU YA 181**
**( Juni 29)**

# Yona Ndani ya Samaki



Yona Alitaka afe au awalipe kisasi Waashuru wakatili. Basi Yona akiwa ndani ya tumbo la samaki akamwomba BWANA. Ila hakuyeyushwa kama chakula! Aliimba Zaburi, alisema "Nalimlilia BWANA kwa sababu ya shida yangu, Naye akaniitikia; katika tumbo la kuzimu naliomba; nawe ukasikia sauti yangu. Maana ulinitupa vilindini, ndani ya moyo wa bahari; Gharika ya maji ikanizunguka pande zote; Mawimbi yako yote na gharika zote zimepita juu yangu. Nami nikasema nimetupwa mbali na macho yako; lakini nilitazama tena kukabili hekalu lako takatifu. Maji yalinizunguka hata nafsini mwangu; vilindi vilinizunguka, Mwani ulikizinga kichwa changu. Nalishuka hata pande za chini za Milima. Hiyo nchi na mapingo yake yalinifunga hata milele; Lakini umenipandisha nafsi yangu kutoka shimoni, Ee BWANA, Mungu wangu. Roho yangu ilipozimia ndani yangu, nalimkumbuka BWANA. Maombi yangu yalikuwasilia, Katika hekalu lako takatifu. Watu waangaliao mambo ya ubatili na uongo hujitenga na rehema zao wenyewe; Lakini mimi nitakutolea sadaka kwa sauti ya Shukrani. Nitaziondoa nadhiri zangu. Wokovu hutoka kwa BWANA."

Basi BWANA mwenye uwezo, anayeweza kuwasiliana na viumbe vyake maana Yeye Ndiye aliyeviumba, akazungumza na samaki amtapike Yona katika pwani ya Ninawi, kule ambako Yona alikuwa hataki kwenda. Ikawa nabii akafika Ninawi kwa usafiri wa samaki badala ya merikebu. Neno la BWANA likamjia mara ya pili tena, "Neno la Bwana likamjia Yona mara ya pili, kusema, Ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa; ukaihubiri habari nitakayokuamuru." Safari hii baada ya matukio ya ajabu, Yona alikuwa tayari kwenda, hata kama ni kwa adui. Akaenda Ninawi kama BWANA alivyomwamuru. Ninawi ulikuwa mji mkubwa, ungetembea mwendo wa siku tatu kuumaliza. Yona akaanza kuingia mjini akipaza sauti yake akisema, "Baada ya siku 40 Ninawi itaangamizwa." Basi watu wa Ninawi wakamwamini Mungu, na wakatangaza kufunga na kujivika nguo za magunia, wakafunga wote,

mkubwa kwa mdogo, kuonesha kujutia dhambi zao. "Habari ikamfikia mfalme wa Ninawi, naye akaondoka katika kiti chake cha enzi, akavua vazi lake, akajivika nguo za magunia, na kuketi katika majivu. Naye akapiga mbiu, akatangaza habari katika mji wa Ninawi, kwa amri ya mfalme na wakuu wake; kusema, Mwanadamu asionje kitu, wala mnyama wala makundi ya ng'ombe, wala makundi ya kondoo; wasile, wala wasinywe maji; bali na wafunikwe nguo za magunia, mwanadamu na mnyama pia, nao wakamlilie Mungu kwa nguvu, naam, na wageuke, kila mtu akaache njia yake mbaya, na udhalimu ulio mikononi mwake." Hii ina maana hata wanyama walifunga. Mahubiri ya nguvu kuliko mahubiri yoyote yaliyowahi kuhubiriwa, alipata 100% ya watu 120,000. Watu pamoja na wanyama! Wakamlilia Mungu kwa nguvu, naam, wakageuka, kila mtu akaacha njia yake mbaya, na udhalimu wa aina yote, maana ni nani "ajuaye kwamba Mungu hatageuka na kughairi, na kuiacha hasira Yake kali, ili msiangamizwe?" alisema mfalme. Mungu akaona matendo yao, kwamba wameziacha njia mbaya, basi Mungu akaghairi Neno lile baya, ambalo alisema atawatenda asilitende. Tunapomwomba Mungu msamaha, kwa toba ya kweli, tunasamehewa na kuanza safari mpya.

Lakini jambo hili lilimchukiza na kumkasirisha Yona. Pengine ataonekana nabii wa uongo, na pia aliona ni maadui zake, na hakupenda Mungu awapende wao, bali Waisraeli tu. Kitabu hiki kinaonesha jinsi upendo wa binadamu ulivyo mdogo sana, na kwamba hatuna huruma na kupendana sisi kwa sisi. Ila upendo wa Mungu hauna kikomo, ni mwingi wa rehema na anasamehe. Akamwambia BWANA, "Ee Bwana; sivyo hivyo nilivyosema, hapo nilipokuwa katika nchi yangu? Hii ndiyo sababu nalifanya haraka kukimbilia Tarshishi; kwa maana nalijua ya kuwa Wewe u Mungu Mwenye neema, umejaa huruma, si mwepesi wa hasira, u mwingi wa rehema, Nawe waghairi mabaya." Sifa kubwa na nzuri hizi za Mungu alizozijua, alitaka ziwe kwake tu, na si kwa watu wengine. Nabii Yona alimwomba Mungu achukue uhai wake haraka kuliko kuona watu wa Ninawi wanasamehewa na kuokolewa. Alikuwa tayari kufa, au aangamie, lakini adui asiokoke. Aliona kuwa kwa sababu haabudu miungu mingine, yupo salama, lakini kumbe alikuwa na dhambi ya kutopenda watu wengine. Upendo ndiyo kanuni kuu ya mbinguni. Kuwapenda adui, ndugu, mke, jirani, wanyama, mimea au viumbe vyote vya Mungu, lakini hasa na zaidi, binadamu aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu. BWANA akamwambia Yona kuwa hafanyi vyema kukasirika. Naye akatoka aende kukaa nje ya mji, akajifanyia kibanda ili aone kitakachoutokea Ninawi, akiwa na shauku ya kuona ukiangamia kama alivyohubiri. BWANA akaweka mtango uliokua siku moja na kumpatia kivuli Yona na kumponya hali yake mbaya.

Yona akafurahia sana ule mtango, ila kulipokucha siku iliyofuata, Mungu aliweka buu likala ule mtango nao ukakatika. Jua likawa kali, likamwunguza Yona, akazimia, naye akajitakia kufa, na kusema, "afadhali nife kuliko kuishi." Mungu akamwuliza Yona kama anafanya vyema kukasirika kwa ajili ya mtango? Akamjibu Mungu kwa hasira, "Ndiyo, natenda vema kukasirika hata kufa." BWANA akamwambia kama wewe una huruma kwa mtango huu ambao hujaufanyia kazi kuukuza na ulikua siku moja na kuangamia siku moja, "Na mimi je? Haikunipasa kuuhurumia Ninawi, mji ule mkubwa; ambao ndani yake wamo watu zaidi ya mia na ishirini elfu, wasioweza kupambanua katika mkono wao wa kulia na mkono wao wa kushoto;

tena wamo wanyama wa kufugwa wengi sana?" Nasi leo tusisite kuwaambia watu wengine habari za Mungu, hata kama wanaonekana ni waovu kiasi gani. Je, mara zingine unajikuta unakimbia kuwaambia watu habari za ufalme wa Mungu, kwamba atakuja karibuni kutoa hukumu? Soma tena kisa cha Yona upate ujasiri.

Kitabu cha Yona kina upekee, kinaonesha upendo mkuu wa Mungu kando ya nchi ya Israeli. Hata watu wa Ninawi walioabudu sanamu na miungu mingine, walikuwa chini ya upendo wa Mungu. Mungu alikuwa tayari kusikia maombi yao na kuwaokoa. Kitabu cha Yona kinaonesha kuwa Mungu ni "Baba Yetu Wote." Wote, iwe ni watoto, wazee, watu wazima, wanyama, warefu, wafupi, matajiri, maskini, weusi na weupe, wote ni wa thamani machoni Pake, japo hawamjui. Hata leo Mungu anaipenda miji, na anataka wakazi wake waokoke. Mungu anaweza kutumia mtu ye yote aliye tayari kupokea wito Wake na kutubu. Basi tusiwe na ubaguzi, chuki, au kiburi wakati Mungu anapotaka kuwaokoa watu wa mataifa mengine, maana hata sisi Mungu ametutoa mbali. Je, hata wewe leo unamkimbia BWANA anapokutuma? Je, unapata hasira na kupenda visasi? Mungu ni wa rehema na, ni Mwenye kusamehe.

Wakati huwezi kukimbia, wakati hauna njia nzuri ya kutoka, omba! Amini moyo wa huruma wa Mungu. Ana njia nyingi za kukuokoa, na kukuweka huru. Acha imani iwe njia yako ya kuchopoka. Acha sifa kwa Mungu iwe pasipoti yako kuwa huru! Kisa cha umishonari wa Yona kinatukumbusha kuwa haitoshi kumfanyia Mungu kazi au kujua mafundisho yote sahihi. Kilicho muhimu ni jinsi mioyo yetu ivyojibu ujumbe Wake Mungu. Wakati Mungu anatuma maonyo magumu, lazima tuwe tayari kuamini na kutii, kutubu na kujirekebisha. Kumjibu Mungu kunahitaji upasuaji wa mioyo yetu na kuiweka wazi. Mungu anatufariji na kila wakati hutoa kile kinachohitajika zaidi, ndio hata kwa wanyama Wake mpendwa. Hebu mioyo yetu ionekane na huruma Yake kila wakati!

Zaburi 37- Ee Bwana, fadhili Zako zafika hata mbinguni, Uaminifu Wako hata mawinguni.6 Haki Zako ni kama milima ya Mungu, Hukumu Zako ni vilindi vikuu, Ee Bwana, unawaokoa wanadamu na wanyama. 7 Ee Mungu, jinsi zilivyo na thamani fadhili Zako! Wanadamu huukimbilia uvuli wa mbawa Zako. 8 Watashibishwa kwa unono wa nyumba Yako, Nawe utawanywesha mto wa furaha Zako. 9 Maana Kwako Wewe iko chemchemi ya uzima, Katika nuru Yako tutaona nuru.10 Uwadumishie wakujuao fadhili Zako, Na wanyofu wa moyo uaminifu Wako.

*Hebu malaika wanaotunza kumbukumbu waandike historia ya mapambano matakatifu na migogoro ya watu wa MUNGU, Hebu na waandike maombi yao na machozi; lakini hebu MUNGU asidharauliwe kwa madai kutoka katika midomo ya wanadamu, yanayosema, "Mimi sina dhambi. Mimi ni mtakatifu." Midomo iliyotakaswa haitatamka kamwe maneno hayo yenye kiburi au dhana potofu.

---

Yona alifanya nini tumboni mwa samaki? Samaki alimtapika wapi Yona? Waliposikia mahubiri, mfalme na watu waliamua kufanya nini? Je, Mungu anathamini wanyama? Utamshaurije mtu anayetesa wanyama ambao hawamdhuru kwa lolote? Ni watu wangapi waliokoka Ninawi? Kisa hiki kinakufundisha nini?

**SIKU YA 182**
**( Juni 30)**

# Kujenga Hekalu

**- Hagai**



Ujumbe wa kitabu hiki ulitolewa wakati wengi wamerudi kutoka uhamishoni Babeli. Nabii Hagai alitumwa kuwatia moyo Wayahudi waliokuwa wamerudi kutoka uhamishoni, kumaliza jukumu la kujenga Hekalu lililokuwa limevunjwa na mfalme Nebukadneza wakati alipouhusuru Yerusalemu. Hagai ni mmojawapo wa manabii ambao ujumbe wake ulisikiwa. Waliposikia, japo walikuwa hawana mali ghafi nyingi, haikupita kitambo wakamaliza kujenga hekalu na Mungu "akawa na watu wake." Hagai na Zekaria wanajulikana kama manabii waliotumwa baada ya kurudi kwao Yerusalemu. Waliandika vitabu vyao wakati wa kurudi kwa mateka wa Yuda, baada ya kuchukuliwa mateka Babeli, na kisha kuwa chini ya Wamedi na Waajemi. Miaka hii ilikuwa ya kukatisha tamaa kwa watu wa Mungu, lakini waliposikia, Roho Wake alifanya kazi. Walirudi wakaona makao yao yamebaki mahame, baada ya miaka 70. Mashamba yalikuwa yameachwa na ingebidi yasafishwe tena, nyumba zilizoharibiwa ilibidi zijengwe, na desturi na mila zao zifundishwe upya na kutekelezwa. Hagai aliwatia moyo wawe na uaminifu kwa Mungu, na wajenge hekalu, maana ni kitovu cha ibada yao, waoneshe kicho, na haki na neema ya Mungu wakati huu mgumu. Akawakumbusha kungojea kuja kwa masihi, ili alete ufalme Wake. Anamwita masihi "Tumaini la vizazi vyote." Kitabu hiki kinaonesha kwamba wote tunahitaji kutiwa moyo na kutia wengine moyo.

Hagai alitumwa na BWANA amwendee Zerubabeli wa ukoo wa kifalme, na Yoshua kuhani mkuu. Akawaambia, "Bwana wa majeshi asema hivi, ya kwamba, Watu

hawa husema, Huu sio wakati utupasao kuja, huu sio wakati wa kujenga nyumba ya Bwana. Ndipo Neno la Bwana lilikuja kwa kinywa cha nabii Hagai, kusema, Je! Huu ndio wakati wa ninyi kukaa katika nyumba zenye mapambo ya mbao, iwapo nyumba hii inakaa hali ya kuharibika? Basi sasa, Bwana wa majeshi asema hivi, Zitafakarini njia zenu." Akawaambia wamepanda mbegu nyingi mashambani bali wakavuna kidogo, wanakula na wala hawashibi, wanakunywa ila kiu haiishi, wanajivika nguo ila hawaondoi baridi, na wakipata mshahara wakiweka kwenye mifuko, inakuwa kama wanaweka kwenye mifuko iliyotoboka, kwa vile hawajaweka kipaumbele kwa Muumba wao. BWANA akawaagiza akisema, "Pandeni milimani, mkalete miti, mkaijenge nyumba, nami nitaifurahia, Nami nitatukuzwa, asema BWANA, mlitazamia vingi, kumbe vikatokea vichache, tena nikavipeperusha mlipovileta nyumbani." Walikuwa wamejilaani, na baraka ziliwakimbia kwa sababu hawajajenga hekalu, na walijijali wenyewe kwa kuishi kwenye nyumba zao za fahari, huku nyumba ya BWANA ikiachwa bila kujengwa. BWANA akasema atazuia mvua, na mazao yasiwe mazuri, na mifugo na vitu vyote vitakuwa havina maendeleo ya kuridhisha.

Ndipo Zerubabeli na Yoshua na watu wakasikia na kuitii sauti ya BWANA, Mungu wao, kupitia kwa nabii Hagai. BWANA akawahakikishia kuwa yupo pamoja nao, basi wakaenda kujenga. Walipomaliza, utukufu wa lile hekalu ulionekana mdogo ukilinganisha na hekalu alilojenga Sulemani, kwa mali na vito vingi. Basi Hagai nabii akapewa Neno kuwaambia kwamba "Nitaijaza nyumba hii utukufu, asema BWANA wa majeshi. Fedha ni mali yangu, na dhahabu ni mali yangu." Akasema kwamba "Utukufu wa mwisho wa nyumba hii utakuwa mkuu kuliko utukufu wake wa kwanza, asema Bwana wa majeshi; na katika mahali hapa nitawapa amani, asema Bwana wa majeshi." Maneno haya yalimaanisha kwamba hekalu hili japo lilionekana halina fahari, YESU atazaliwa na kuabudu kwenye hekalu hilo. Na ndio utukufu mkubwa zaidi ya hiyo dhahabu ya Sulemani au fahari ya mapambo. Yaani ni Mungu pamoja na watu. Kitu hakiwezi kuwa kitakatifu bila Mungu kukifanya kitakatifu.



BWANA akawaambia kuwa vile vitu najisi haviwezi kufanywa visafi kwa vikigusa vitu vitakatifu ndiyo hivyo ambavyo hekalu haliwezi kuwa na ndumba ya kumtakasa mtu mwovu, eti bora wako hekaluni. Yaani jengo la hekalu si mbadala wa kuishi maisha ya imani na utakatifu. Utakatifu unatokana na kujitoa wakfu kwa Mungu na kushika amri Zake

Hagai anamaliza ujumbe wake kwa kumwambia Zerubaeli na Yoshua kwamba Mungu amewaweka katika cheo hicho kwa sababu maalum, na watakuwa mbaraka kwa watu Yeye akiwa hapo. Basi tutafute ufalme na haki ya Mungu na yote hayo ambayo hata mataifa wanayatafuta sisi tutazidishiwa. Je, kanisa lako linafanana na nyumba unayoishi? Nyumba ya ibada yapaswa iwe bora kupita nyumba unayoishi. Endapo unaabudu chini ya mti, bali wewe unakaa katika jumba la fahari, ni wakati wa kujiuliza na kubadili sifa hiyo.

*Malaika husikia sifa zinazotolewa na ombi la imani, na hupeleka maombi kwa Yeye ambaye huhudumu katika Patakatifu kwa ajili ya watu Wake, na kuombea wema na haki Yake kwa niaba yao. Ombi la Kweli humshikilia Mweza wa yote, na huwapa wanadamu ushindi. kwa kupiga magoti yake, Mkristo hupata nguvu za kukinzana na vishawishi.

---

Ujumbe wa Hagai unahusu nini? Watu waliposikia ujumbe wa Hagai nini kilitokea? Ni viongozi gani walishughulika na ujenzi? Kwa nini ni vyema kanisa la Mungu kuonekana zuri kama kwako au zaidi? Nini maana ya tumaini la vizazi vyote?

**SIKU YA 183**
**( Julai 1)**

# Ujumbe wa Nabii Nahumu



Nahumu alitoa ujumbe wake juu ya Ninawi, mji mkuu wa ufalme wa Ashuru. Nahumu ina maana fariji au faraja.

Ilikuwa imepita miaka 150 toka Yona Aende ninawi na kuuonya juu ya hukumu iliyokuwa inaukabili. Watu wa Ninawi waliungama na wakaacha uovu wao. Mfalme, mifugo na watu wote walifunga na kutubu. Safari hii nabii Nahumu alitumwa kuwaonya tena Ninawi, kwamba itaangamizwa kwa moto milele isiinuke tena kwa ajili ya ukatili, na kuabudu miungu mingine. Safari hii Ninawi hawakusikiliza. Nah. 1:7, 8, 11, 14.

Nahumu anatwambia kuwa BWANA ni Mungu Mwenye wivu, Naye hujilipiza kisasi; Naye ni mwingi wa hasira kwa waovu, wale wanaofanyia wengine ubaya watapata akiba ya hasira Yake. Mungu ana uwezo wote, aweza kuikemea bahari na kuikausha, anaweza kuihamisha milima na hata dunia hutetemeka mbele Zake. Yeye ni ngome au kimbilio letu wote tunaomtegemea. Ahadi ya ajabu, tunaambiwa mbinguni dhambi haitainuka mara ya pili. Kama kuna ahadi ya ajabu ni hii, Je! waweza kupiga picha ya maisha bila dhambi kabisa? Ahimidiwe Mungu, hii ina maana marafiki zetu, ndugu zetu, sisi wenyewe tutakuwa tunatendeana na kuwaziana mema tu, saa 24 zote! Nimeuhesabu huu kama mwujiza mkubwa sana. Hata mara nyingi nimeomba utokee katika moyo wangu sasa, kwamba nisifanye dhambi tena, na kumhuzunisha Mungu.

Watu wa Ninawi wasioweza kumsikiliza Mungu waliambiwa kwamba watakuwa

kama walevi wakiyumba yumba bila msimamo. Mungu ataangamiza watoto na pia miungu ya Ashuru. Bali mtu apelekaye habari njema za Mungu na atangazaye amani, ana miguu mizuri.

Mungu anaahidi kuirudisha fahari ya Yakobo toka kwa Ninawi, maana watu wa Ninawi wameiharibu Israeli. Nyumba ya mfalme wa Ninawi imeyeyushwa, atachukuliwa na wajakazi wake watalia wakipigapiga vifua vyao. Watakimbia wala hakuna atakayetazama nyuma, itakuwa na utupu, ukiwa na uharibifu. Mioyo ya watu itayeyuka na magoti kugongana, kutakuwa na uchungu usoni pa watu wote kwa hofu. Mungu atawakatilia mbali mawindo yake, katika nchi na sauti ya wajumbe Wake hazitasikika kamwe.

Mji wa Ninawi ulijaa damu, ole wake maana kulikuwa na uongo na unyang'anyi. Kelele za vita, mijeledi, magari ya farasi na upanga na mikuki inayometameta huonekana. Watu wengi watauawa na mizoga mingi itazagaa kwa sababu ya wingi wa ukahaba, ukahaba wa mambo ya uchawi. Ninawi aliambiwa atafunuliwa mbele ya watu na kuwaonesha mataifa utupu wake na falme zingine aibu yake. Mungu atatupa uchafu wa Ninawi na machukizo yake, na atakuwa si kitu, watu watamtazama kwa dharau. Watu watazamao Ninawi watakimbia na kusema Ninawi imeharibika, ni nani atakayeuhurumia mji huu. Wafariji hawatapatikana kwa mji huu.

Ninawi aliambiwa hakuwa na nguvu. Waamoni, Misri, Ethiopia, Putu na Libya zilimsaidia, lakini alichukuliwa mbali, akaenda utumwani, watoto wake wachanga waliteswa, watu wenye heshima wakapigiwa kura na kuuzwa kwenye makutano ya njia. Wakuu wake walifungwa minyororo.

Ngome za Ninawi zitakuwa kama mitini inayoanguka, watakaobaki ni wanawake tu kwenye malango. Maji yatakuzingira, moto utakuteketeza, upanga utakukatilia mbali na tunutu atakumeza. Japo una wafanyabiashara wengi kama nyota, tunutu wataharibu na kisha kuruka na kwenda zao. Majemedari wako watakuwa kama makundi ya panzi, watuao katika vitalu siku ya baridi, lakini jua lipandapo huruka na kwenda zao, na mahali pao hapajulikani.

Wachungaji na walinzi wake mfalme wa Ashuru watakuwa wanapiga usingizi tu na watu wenye heshima wanapumzika ila watu watatawanyika na hakuna atakayeweza kuwakusanya. BWANA akasema kwamba jeraha za Ashuru zitakuwa kubwa na hazitapungua na watu watakaosikia watapiga makofi kushangilia kwani hakuna ambaye Ashuru haikumfanyia ukatili.

Mungu ni hapendi wale ambao wanaodharau na kupuuzia ombi Lake la kuacha njia zao mbaya, Yu dhidi ya wale ambao wanawakandamiza wenzao bila huruma, na dhidi ya wale ambao wanaendelea kuwa na mioyo migumu. Mungu, hata hivyo, Yuko tayari kwa wale ambao wako tayari kuongozwa na Roho Wake na Yeye huwarejesha ! Je, wewe nasimama wapi leo?

*MUNGU hawaachi watoto Wake wapotovu walio dhaifu katika imani, na wanaofanya makosa mengi. Bwana husikiliza na kusikia maombi yao na ushuhuda wao. Wale wanaomtazama Yesu siku kwa siku na saa kwa saa, wanaokesha kwa maombi, wanamkaribia Yesu. Malaika walio na mbawa zilizochanuliwa hungoja kupeleka sala zao za toba kwa MUNGU, na kuzisajili katika vitabu vya mbinguni.

---

Nahumu alitoa ujumbe wake kwa watu gani? Kuna tofauti gani kati ya matokeo ya kazi ya Yona na Nahumu? Dhambi ya watu wa Ninawi ilikuwa ipi?

**SIKU YA 184**
**( Julai 2)**

# Obadia siku ya BWANA



Obadia ni kitabu kingine cha unabii mfupi katika Agano la Kale. Obadia ina maana mtumishi wa Mungu. Kitabu hiki kinazungumzia uhusiano wa Israeli na Edomu. Edomu alikuwa ndugu wa Israeli, maana walikuwa ni uzao wa Esau aliyekuwa ndugu ya Yakobo. Obadia anasema Edomu itaanguka kwa ajili ya kiburi cha usalama inayofikiria inao. Walifurahia wakati Israeli inatekwa. Mungu akasema, Siku ya BWANA inakuja na nyumba ya Yakobo itakuwa mwali wa moto, na nyumba ya Edomu itakuwa mabua makavu, nao watawaka kati yao, na kuwateketeza, wala hatasalia mtu awaye yote katika nyumba ya Esau, kwa kuwa BWANA amesema hayo. Hata leo BWANA anasema "Nitawalaani wakulaanio, na kuwabariki wakubarikio." Maamuzi yetu tunayofanya yanaweza kutugharimu au kutubariki. Edomu anaambiwa kwamba wezi wanaiba wanachobeba tu, ila Edomu itakapovamiwa, hakuna kitakachobaki. Hata wale wanaochuma zabibu, wataacha patupu. Maana wanafurahia Edomu iliyofurahia maanguko ya Israeli.

Obadia anaonesha kuwa Mungu atahukumu Edomu, ambao wamekuwa adui kwa Israeli watu Wake na kuwafanyia ubaya. Mungu atawatetea Israeli. Wakati mfalme Nebukadreza alipovamia Yuda, Edomu alisaidia kuteka nyara miji. Edomu anaambiwa akumbuke, kwamba damu ni nzito kuliko maji. Obadia kinaeleza kwa nguvu kwamba Mungu Ndiye Hakimu mkuu na ataondoa ubaya wa Edomu. Anasema "siku hiyo nitawaangamiza watu wenye akili katika Edomu, na wenye ufahamu katika kilima cha Esau … mashujaa watafadhaika, na kuuawa kilima cha Esau."

Hata leo inabidi tuwe waangalifu, tukiwaona adui zetu wakipata shida, tusifurahi au kucheka, bali tuwe tayari kuwasaidia, kwa mahitaji yao, iwe ni chakula, mavazi au malazi. Mungu Ndiye analipiza kisasi na siyo sisi binadamu. "Kwa maana hiyo siku ya Bwana i karibu juu ya mataifa yote; kama ulivyotenda, ndivyo utakavyotendwa; malipo yako yatakurudia juu ya kichwa chako mwenyewe." Basi leo tunaingoja siku ya BWANA na dalili zinatuonesha kuwa i karibu sana. Hebu tumwombe Mungu ili siku hiyo iwe siku ya tumaini lenye baraka kwetu, na kisha tuseme "Tazama huyu Ndiye BWANA tuliyekuwa tumemngojea." Mambo haya yaliwapata wao ili kuwa

mfano kwetu, nayo yakaandikwa ili kutuonya sisi tunaoishi mwisho wa wakati. Je, umejifunza kwa mifano ya wana wa Israeli? Je, unataka ubadilishe nini ili uwe mtiifu leo?

Wakati Wababeli waliposhambulia Yerusalemu, Waedomu waliona nafasi yao ya kuwamaliza na adui wao wa kihistoria. Obadiah 1: 10-16 inaonyesha mifano ya jinsi walivyofanya hivyo: Walifurahi kama Yerusalemu walipoanguka, walijiunga na Wababeli katika shambulio lao dhidi ya Yerusalemu, waliwakata wale ambao walijaribu kutoroka na kuwapa waathirika kwa Wababeli. Waliwadhihaki Waisraeli ambao walikuwa kwenye shida.

Kwa nini walifanya hivi? Labda waliamini kuwa hakukuwa na tumaini tena kwa Israeli na kwamba Mungu amekamilika nao. Je! Unafurahi kwa maafa ya wengine? Je! Unalipa mema na uovu na unashangaa kuwa uovu haujawahi kuondoka kutoka nyumbani kwako? (Prov 17:13). Au unaweza kuwa katika msimamo wa Israeli leo, ukishangaa Mungu Yuko nawe katika maafa yako. Ndiyo Yuko karibu. Mwishowe, Mungu aliadhibu Waedomu kwa dhambi yao na akarudisha Israeli (ob. 1:21).

*Malaika Wanangoja Kujibu Maombi Yetu—Mara nyingi katika kujali wanaoteseka, uangalifu mwingi unatolewa juu ya mambo madogomadogo, huku hitaji la wagonjwa la zile Kweli zote kuu za wokovu wa injili, ambazo zitahudumu kwenye roho na mwili, zimesahaulika. Unapopuuza kuwaombea wagonjwa, unawanyima baraka kubwa; kwa maana malaika wa MUNGU wanangoja kuhudumu kwenye nafsi hizi katika kuitikia maombi yako.

---

Obadia ina maana gani? Edomu ina shida gani? Kwa nini mambo ya watu hawa yameandikwa kwetu sisi watu wa leo? Siku ya BWANA ina maana gani?

**SIKU YA 185**
**( Julai 3)**

# Habakuki – Anamwuliza Mungu Maswali ili apate Tumaini, akiona Kimya anamwuliza "Hutafunga goli tena?"

Nabii Habakuki anasemekana kuishi miaka ya mwishoni ya ufalme wa Yuda, kabla Yuda haijaanguka. Wahusika wakuu katika kitabu hiki ni Habakuki na Wakaldayo ambao walijulikana kama Wababeli. Habakuki japo ni kitabu kifupi, nia yake ni kueleza juu ya hukumu. Mungu anasema dhambi ya Yuda ni kubwa. Kitabu hiki ni tofauti na vingine kwani Habakuki anazungumza na Mungu kuhusu watu, na si kama manabii wengine wanazungumza na watu kuhusu ujumbe wa Mungu. Habakuki anashangaa kwamba nchi zote mashuhuri zilianguka, na watu hawakuamini, na Babeli ikatawala kila kitu. Lalamiko lake la kwanza ni "Nilie hata lini, wewe usitake kusikia?" Anamlilia BWANA kwa sababu ya udhalimu, uovu, ukaidi, ugomvi, uharibifu na mashindano. Sheria ya BWANA imelegea, na watu wanakosa haki yao, kwa sababu ya rushwa, hukumu imepotoka. Mungu alisema, "Angalieni, enyi mlio kati ya mataifa, katazameni, kastaajabuni sana; kwa maana Mimi natenda tendo siku zenu, ambalo hamtaliamini hata mkiambiwa. Kwa maana, angalieni, nawaondokesha Wakaldayo, taifa lile kali, lenye haraka kupita kiasi; wapitao katikati ya dunia, ili wayamiliki makao yasiyo yao. Hao ni watu wa kutisha sana, wa kuogofya sana; hukumu yao na ukuu wao hutoka katika nafsi zao wenyewe. Farasi zao ni wepesi kuliko chui, ni wakali kuliko mbwa-mwitu wa jioni; na wapanda farasi wao hujitapa naam, wapanda farasi wao watoka mbali sana; huruka kama tai afanyaye haraka ale." Hata leo tunashangaa, uovu mwingine watu wanaotendewa na kusema, "mbona Mungu yupo kimya." Mungu alinyamaza vile vile mwana wake akiwa msalabani, ili atuokoe japo alikuwa na uwezo wote.



Swali lake la pili Habakuki aliuliza, "Wewe uliye na macho safi hata usiweze kuangalia uovu, wewe usiyeweza kutazama ukaidi, mbona unawaangalia watendao

kwa hila; na kunyamaza kimya, hapo mtu mwovu ammezapo mtu aliye mwenye haki kuliko yeye; na kufanya wanadamu kuwa kama samaki wa baharini, kama vitu vitambaavyo, ambavyo havina mtawala?" Habakuki akasema atasimama kwa zamu yake na kungoja aone BWANA atakavyojibu swali lake au malalamiko yake. Anasema,"Bwana akanijibu, akasema, Iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji. Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulio amriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia. Tazama, roho yake hujivuna, haina unyofu ndani yake; lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake." Martin Luther, mwanamatengenezo wa Ujerumani, alipogundua Ukweli huo, aliwasaidia Wakristo wengi "kuwekwa huru."

Habakuki aliambiwa awe mvumilivu, na kumtumaini Mungu japo hakuelewa vizuri mambo yalivyokuwa yakiendelea au kwamba yatakuwa na tamati gani. Habakuki anatoa ole kwa wale wanaoongeza kisicho mali yao, au kumwaga damu, au kupata mapato ya uovu, au kumpa jirani yake pombe au sumu ya kuwalevya ili waone aibu yao. Habakuki anakumbusha kicho kwa Mungu akisema, "BWANA Yumo katika hekalu Lake takatifu, dunia yote na inyamaze kimya mbele Zake." Yeye ni Mweza wa yote.

Habakuki anatamka sala yake akisema, "Ee Bwana, nimesikia habari zako, nami naogopa; Ee Bwana, fufua kazi yako katikati ya miaka; Katikati ya miaka tangaza habari yake; Katika ghadhabu kumbuka rehema." Habakuki akaona hakuna jema kama vile kumtegemea na kumngojea BWANA. Anamalizia kwa matumaini akisema, "Hata kama mtini hatuchanua maua, wala mzabibu hautakuwa na matunda,… Na mashamba hayatatoa chakula, Zizini hamtakuwa na kundi, wala vibandani hamtakuwa na kundi la ng'ombe. Walakini nitamfurahia BWANA nitamshangilia Mungu wa wokovu wangu. YEHOVA aliye BWANA, ni nguvu zangu, Yeye hufanya miguu yangu kuwa kama ya kulungu, Naye ataniendesha katika pahali palipoinuka." Habakuki akaridhika kwamba japo mambo yaweza kuonekana magumu na mabaya, Yeye ataegemea kwa BWANA na kuwa mgeni wa BWANA maana kuna nafuu na kupona kwa BWANA."

Habakuki anatufundisha kwamba tunaweza kumwuliza Mungu, ila kwa heshima na kicho. Mara nyingi hatujui ni nini kinaendelea nyuma ya pazia, iwe ni shida za wazazi wetu, mambo yanayohusu shule au marafiki zetu, mara zingine tunaweza kupata shida na mambo yakawa ni magumu. Tunaweza kuona adui anashinda nasi tunashindwa, lakini bado Mungu ni mkuu na anatawala. Tutulie na kuwa wavumilivu, tukijua kuwa anafanya yote kwa wema kwa ajili yetu. Mungu hutunza ahadi, Yeye ni mwaminifu. Mamlaka yote ni Yake, hivyo tutulie Kwake na kuwa na imani. Lazima tujipumzishe Kwake na kumtumaini. Kitabu cha Habakuki kinaishia kwa zaburi au wimbo wa kumtukuza Mungu maana atawaokoa watu Wake.

Habakuki aonyesha kukasirishwa na jeuri na ukosefu wa haki, naye anatufundisha kwa kila kinachotuhangamisha moyo, twende kwa Mungu.

Tunapokaribia mwisho wa historia ya dunia, maswali aliyouliza Habakuki yanafanana na maswali tunayopambana nayo leo. Kama huyu nabii, tumekuwa tukimuomba Mungu aingilie kati na kukomesha maumivu, mateso na maovu yanayotujia kutoka pande zote. Mungu hajakuwa mzembe au asiyetenda katika siku za Habakuki, hata leo Yeye si asiyetenda jambo. Hebu tumwamini Yeye.
Tukumbuke kuwa Mungu mara nyingi hutumia vyanzo visivyowezekana ili kutimiza mapenzi yake. Hatutaelewa daima mafumbo ya njia Zake, lakini tunapaswa kuwa na hakika kwamba mioyo yetu ni safi, na mikono yetu ni safi. Nguvu Zake ni za milele, na Kwake siku moja ni kama miaka elfu. Wakati huo huo, hebu tuitikie amri, "Bwana Uu ndani ya hekalu lake takatifu; dunia yote na ikae kimya mbele zake" na tuwe na shukrani kwamba tunaweza kumfikia mara moja na kibinafsi. Na tufurahie usikivu Wake maalum na tutulizwe na Roho Wake wa Neema. Imani safi kama hii na mbichimbichi ni nadra kuonekana na watoto wa Mungu, lakini hapa inamiminwa kwa uhuru.

**Siku baada ya siku mzozo kati ya wema na uovu unaendelea. Kwa nini wale ambao wamepata fursa nyingi na manufaa hawatambui uzito mkubwa wa kazi hii? Wanapaswa kutumia akili katika suala hili. MUNGU Ndiye Mtawala. Kwa uweza Wake mkuu Yeye huwadhibiti na kuwaongoza watawala wa kidunia. Kupitia mawakala Wake Anafanya kazi ambayo iliamriwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

---

Kwa nini kitabu cha Habakuki ni tofauti na manabii wengine? Swali la kwanza la Habakuki ni nini? Swali lake la pili ni nini? Je, kwa nini kumwuliza Mungu kinachoendelea ni muhimu kwetu?

**SIKU YA 186**
**( Julai 4)**

# Ujumbe wa Sefania



Nabii Sefania aliandika kitabu mwaka 630KK. Sefania alizaliwa, wakati huu wa uovu, na BWANA alionekana kuwa kimya na kwamba hatafanya jema wala baya. Mungu alimwinua nabii Sefania ili kuwaeleza watu kuwa hukumu itakuja na kuwaambia watubu kabla ya ufalme wa Yuda kuanguka. Mungu anasema ufalme wa kusini wa Yuda una uovu. Mungu akamtuma Sefania kuwa msemaji wake kuwaonesha watu bendera ya hatari na maonyo ya kubadili njia zao. Waliitwa wamtafute BWANA maadamu anaonekana. Akawaambia siku ya BWANA i karibu, na inafanya haraka, na hata shujaa atalia kwa uchungu mwingi, itakuwa siku ya ghadhabu, dhiki na fadhaa, siku ya uharibifu na ukiwa, siku ya utusitusi na mawingu na giza kuu. Siku hiyo pia mali haitaweza kuwaokoa nao watazitupa barabarani mtu asiweze kuokota, maana thamani yake itakuwa imekwisha.

Sefania Akawaambia, "Basi kama niishivyo, asema Bwana wa majeshi, Mungu wa Israeli, Hakika Moabu atakuwa kama Sodoma, na wana wa Amoni kama Gomora, yaani, milki ya upupu, na mashimo ya chumvi, ukiwa wa daima; watu wangu waliosalia watawateka nyara, na watu wa taifa langu waliobaki watawarithi. Mambo hayo yatawapata kwa sababu ya kiburi chao, kwa kuwa wamewatukana watu wa Bwana wa majeshi, na kujitukuza juu yao. Bwana atakuwa Mwenye kuwatisha sana; kwa maana atawafisha kwa njaa miungu yote ya dunia; na watu watamsujudia Yeye, kila mtu toka mahali pake; naam, nchi zote za mataifa. Na ninyi Wakushi pia, mtauawa kwa upanga Wangu. Naye atanyosha mkono Wake juu ya upande wa kaskazini, na kuiangamiza Ashuru; Naye ataufanya Ninawi kuwa

ukiwa, kuwa mahali pakavu kama jangwa."
Mungu anawaita watu kutafuta haki na unyenyekevu, wakati muda ungalipo. Wasiseme kesho, kesho, mwishowe ikawa wamechelewa. Mungu atafisha miungu yao kwa njaa, na watu watamsujudu Yeye. Hebu tuwe na toba ya kweli sasa maadam mlango wa rehema uko wazi, tuache uovu maana siku ya hukumu yetu inakuja karibuni na mlango wa rehema karibuni utafungwa milele.

Maneno haya ya kutia moyo kabisa katika kitabu hiki ambayo tumeshayazungumzia yanapaswa kukaririwa na kila mtu "Bwana, Mungu wako, Yu katikati yako shujaa awezaye kuokoa; Atakushangilia kwa furaha kuu, Atakutuliza katika upendo Wake, Atakufurahia kwa kuimba". Furaha ya upendo wa Mungu ni kuimba kuhusu sisi. Hakika hili ni jambo la ajabu!

Kitabu hiki kinaonyesha ushindi! Hata pale Bwana ashukapo ili "kufagia kila kitu" (1:1) katika hukumu, tunaelewa kwamba hukumu ni habari njema, na hatuhitaji kuogopa. Sefania anatazama chini katika historia na kuona wakati ambapo mabaki ya Bwana yatakusanywa kutoka kila sehemu ya ulimwengu. Anaonyesha kutakuwa na wawakilishi kutoka "ng'ambo ya mito ya Ethiopia" . Sisi tunaoishi karibu na Ethiopia tunapata furaha kwamba hapo ni nyumbani! Je, ni nini ajenda ya hawa masalio waliokusanywa? Ni Kumwabudu Mungu!

Umati huu wa tamaduni nyingi unapokusanyika pamoja, Mungu huwaita "waabudu wangu" na kwa kweli Yeye hufurahi "juu yao kwa kuimba" (3:17). Itakuwa siku ya ajabu kiasi gani kumsikia Mungu Mwenyewe akiimba! Mungu anatoa ahadi saba zenye nguvu na za kibinafsi kwa masalio. Ataondoa huzuni, atashughulika na wale waliowadhulumu, ataokoa vilema, atawapa sifa na heshima, atawakusanya, na kuwaleta nyumbani na kurejesha baraka zao mbele ya macho yao wenyewe.

Je, ahadi yoyote kati ya hizi saba inazungumzia hali yako ya sasa? Je, unahisi huzuni, kukandamizwa, woga, na hata dhaifu? Bwana anasema "Basi, ningojeeni" Nije! Anakuja kutimiza ahadi hizo kwa ajili yetu, nasi tutamwabudu milele. Hakika nasikia kurukaruka kama swala!

Mungu anawakumbusha kwamba huwapa wenye dhambi kila wasichostahili, yaani huruma Zake. Sefania anasema kutakuja siku za matumaini, masalio wa Israeli watatoka utumwani, chini ya ulinzi wa BWANA na kutimiza ahadi Yake. Hawa mabaki ya Israeli hawatasema uongo, wala ulimi wa kuhadaa hautaonekana kwao. Siku hiyo BWANA ataondoa hukumu zao. Mungu atawalipa wale wanaowatesa Israeli, na kila achechemeaye atamponya, naye aliyefukuzwa atamkusanya na kumrudisha, Mungu ataingiza na kuwakusanya na kuwa na jina miongoni mwa watu wa dunia nzima.

---

Ujumbe mkuu wa Sefania ni upi? Nani tumaini letu la kututoa katika uovu wetu? Mali zina nafasi gani ya kutuokoa siku ya hukumu? Watu wa Mungu waliambiwa watafute nini? Kwa nini kutafuta haki na unyenyekevu ni muhimu? Je, unaweza kuandika beti moja la wimbo ambao Mungu ataimba kuhusu sisi!?

**SIKU YA 187**
**( Julai 5)**

# Zekaria-Ujumbe kwa Waliorejea Toka Uhamishoni



Mnamo 520 B.K. Bwana alimwita Zekaria kuungana na Hagai ili kuwaamsha Wayahudi waliokuwa wamerudi Yerusalemu kutoka utumwani Babeli. Miaka kumi na sita ilikuwa imepita tangu Zerubabeli arudi nao kwenye nchi yao ya ahadi. Sikukuu ya Vibanda iliadhimishwa. Kisha, msingi wa Hekalu uliwekwa.

Kisha shida ikatokea kutoka kwa watu walio karibu nao. Kazi ilisimamishwa. Nabii Hagai aliwaongoza kufanya upya juhudi zao za kukamilisha utume ambao Mungu alikuwa nao kwao - ujenzi wa Hekalu.

Somo hili ni kwa ajili yetu. Usalama wetu uko kwa Mungu. Tunapaswa kuamini maneno Yake. Ujumbe wa yule mtu aliyepanda farasi mwekundu, "dunia imetulia," unarejelea uhakika wa kwamba pambano kuhusu ufalme wa Uajemi lilikuwa limekwisha. Dario mfalme mpya aliwapendelea Wayahudi zaidi. Bwana akasema, Narudi Yerusalemu, nyumba yangu itajengwa. Watu Wake walipaswa kukamilisha misheni ambayo kwa ajili yake alikuwa amewarudisha. Pembe nne zinafafanuliwa kuwa zile zilizofanya kazi dhidi ya watu wa Mungu. Wale maseremala-mafundi wanne, wanarejelea Zerubabeli, Nehemia, Hagai, na Zekaria.

Kutoka kwenye miti miwili ya mizeituni, mafuta ya dhahabu yalimwagwa kupitia mirija ya dhahabu kwenye bakuli la kinara, na kutoka humo ndani ya taa za dhahabu zilizotoa mwanga kwa Patakatifu. Kwa hiyo kutoka kwa watakatifu wanaosimama katika uwepo wa Mungu, Roho Wake anakabidhiwa kwa vyombo vya kibinadamu ambavyo vimewekwa wakfu kwa utumishi Wake. Kazi ya watiwa-mafuta hao wawili ni kuwasilisha nuru na nguvu kwa watu wa Mungu. Ni kupokea baraka kwa ajili yetu kwamba wanasimama katika uwepo wa Mungu.

Zekaria ina maana Mungu anakumbuka. Ujumbe wa Zekaria unatwambia kuwa tukiwa bado tuna pumzi, tusikate tamaa, kwani bado tuna tumaini la kumchagua BWANA na kuishi milele. Japo waliadhibiwa kwa uovu wao, lakini ulikuwa ni wakati wa kumrudia Mungu, na kuwa waaminifu. Zekaria, Yoshua, Zerubabeli, Hagai waliishi wakati mmoja. Mungu anawaambia watu wamtumikie sasa, siyo kesho. BWANA anasema, "Nirudieni, Nami nitawarudia." Watu walifurahi kurudi Yerusalemu toka utumwani Babeli. Hata hivyo walikuwa na wasiwasi kwamba hawatakuwa salama, au maadui watawavamia. Walijiuliza kama Mungu amesahau uovu wao wa zamani, au wataendelea kupata adhabu kwa yale yaliyofanya wakachukuliwa mateka? Mungu anawaambia kwamba hakupendezwa na mataifa mengine yalivyowafanyia ukatili, japo Waisraeli walikosa, ila mataifa haya yamekuwa katili mno kwao. Ingawa Mungu aliwahurumia, lakini walipaswa wawasikilize manabii.

Zekaria anaonesha kuwa Mungu anaulinda Yerusalemu na kwamba Zerubabeli atamaliza kazi ya kujenga hekalu; si kwa uwezo wake bali kwa uwezo wa Roho wa Mungu. Hata Tatenai alipokuja kusitisha kazi, Zerubabeli alimwambia wao ni watumishi wa Mungu wa mbingu na nchi, na wanamjengea nyumba yake. Walipowashtaki kwa Dario, mfalme aliagiza kuchunguza kumbukumbu na kukuta kuwa Koreshi aliwaruhusu kujenga hekalu, hivyo akatuma ujumbe kwa Tatenai, kuwa aache kuharibu kazi ya kujenga nyumba ya Mungu. Mfalme akasema wapewe hata mali ghafi, chakula na msaada ili wamalize ile kazi.

Yoshua, kuhani mkuu, anasimama mbele za BWANA na Shetani anataka kumpinga. Lakini BWANA anamtolea Yoshua utetezi na kuamuru avuliwe mavazi machafu na kumvika mavazi safi. BWANA akamwambia Shetani, "Bwana akamwambia Shetani, Bwana na akukemee Ewe Shetani; naam, Bwana, aliyechagua Yerusalemu, na akukemee; je! Hiki si kinga kilichotolewa motoni? Yerusalemu ni kinga cha moto kilichopona, kilichookolewa kisiungue. Mungu akamwambia, "Tazama nimekuondolea uovu wako, Nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi. Yoshua anaambiwa kuwa ikiwa atatembea katika njia za BWANA, basi atapewa nafasi ya kuhukumu nyumba ya Mungu. Zakaria anaona njozi ya taa saba na miti miwili ya mizeituni, na anamwambia Zerubabeli kuwa atamaliza kazi ya kujenga hekalu, si kwa uwezo wala si kwa nguvu za binadamu, bali ni kwa roho wa Mungu.

Nabii anahimiza kutenda wema kwa yatima, wajane na wageni, ila dini yetu isiwe tu ya kusaidia watu wenye mahitaji kama ustawi wa jamii, bali ya kumpenda Mungu kwa moyo, nguvu, roho na akili zetu zote, na jirani kama nafsi yako.

BWANA anasema kuwa Yuda ilikuwa laana lakini sasa itakuwa baraka. Unabii wa Masihi unaonekana mara kadhaa, mfano - kupanda mwana punda kama mfalme; kuuzwa kwa vipande 30 vya fedha, pia, “watamwona waliyemchoma,” “BWANA atainua ‘Chipukizi’, na mtumishi wake. Hata kusulibishwa Kwake Yesu – jeraha, “Je! jeraha hizi ulizo nazo kati ya mikono yako ni nini?” Naye atajibu, “ni jeraha nilizotiwa katika nyumba ya rafiki zangu.” Yesu alitiwa jeraha na rafiki Zake. Hata unabii wa siku za mwisho umo pia, kama huu, “siku hiyo miguu Yake itasimama juu ya mlima wa mizeituni nao utapasuka katikati Yake.”

Unabii wa Zekaria umejumuisha kuja kwa Yesu mara ya kwanza, alipozaliwa na ujio wa mara ya pili, atakapokuja kutuchukua kwenda mbinguni. Je, unapanga kuwapo katika Yerusalemu mpya? Hebu fumba macho na kumuomba Mungu ili akutayarishe uwe pale siku hiyo.

*Laiti sote tungeweza kutambua ukaribu wa mbingu na dunia! Watoto waliozaliwa duniani hawalijui hili, kwamba wana malaika wa nuru kama webzu ba walinzi wao; kwa maana wajumbe wa mbinguni wanatumwa kuwahudumia wale ambao watakuwa warithi wa wokovu. Shahidi wa siri hulinda kila nafsi inayoishi, akitafuta kushinda na kuivuta kwa Kristo. Malaika hawamwachi kamwe yule anayejaribiwa kuwa mawindo kwa adui ambaye ataangamiza roho za watu ikiwa ataruhusiwa kufanya hivyo. Maadamu kuna tumaini, mpaka watakapompinga Roho Mtakatifu kwa uharibifu wao wa milele, wanadamu wanalindwa na walinzi wa mbinguni.

---

Mungu alitoa wito gani kwa watu Wake? Zerubabeli na Yoshua walikuwa nani? Yoshua kuhani aliposimama mbele za Mungu, ni nini kilitokea? Kwa nini ni muhimu kujua kuwa kazi ya Mungu haifanywi kwa uwezo au nguvu zetu, bali kwa uwezo wa Mungu?

**SIKU YA 188**
**(Julai 6)**

# Malaki – Ujumbe wa Matengenezo, Bwana Atafungua Madirisha na si Milango!



Kitabu cha Malaki ndicho cha mwisho kwenye Agano la Kale. Ilipita miaka 400 mpaka kufikia kipindi cha Agano jipya. Malaki ina maana 'mjumbe wa Mungu.' Mungu anawakumbusha watu Wake kwamba majukumu ni muhimu. Watu hawa wanakuwa kama wanamwambia BWANA kuwa anawasingizia kwa mambo ambayo hawakufanya. Wanamwuliza Mungu maswali.

Mungu anawaambia "Nimewapenda ninyi" nao wanajibu "Umetupendaje?" Mungu anawaambia "mmelidharau Jina Langu" nao wanajibu "tumelidharau Jina Lako kwa jinsi gani?" BWANA anasema "nirudieni Mimi, asema BWANA wa majeshi" watu wanasema "turudi kwa namna gani?".

"Je, mwanadamu atamwibia Mungu?", watu wanajibu "tumekuibia kwa namna gani?" Mungu anasema "mmemchokesha BWANA kwa maneno yenu" wanajibu "Tumemchokesha kwa maneno gani?"

"Bwana wa majeshi awauliza ninyi, enyi makuhani, mnaolidharau Jina Langu. Nanyi mwasema, Tumelidharau Jina Lako kwa jinsi gani? Mnatoa chakula kilichotiwa unajisi juu ya madhabahu yangu Nanyi mwasema, Sisi tumekutia unajisi kwa jinsi gani? Kwa sababu mwasema, Meza ya Bwana ni kitu cha kudharauliwa." Mungu anasema mmelitia unajisi hekalu, BWANA anasema "sina furaha kwa ajili yenu," afadhali mlango ungefungwa ili msije mkawasha moto bure madhabahuni Pangu kwa kutoa kafara za kutoniheshimu "kwa maana tokea mawio ya jua hata machweo yake, Jina Langu ni kuu katika mataifa…" Mungu anasema mtoto humheshimu

baba yake, na mtumishi humheshimu bwana wake, “kama Mimi ni Baba yenu, heshima Yangu iko wapi?” BWANA anasema kuwa makuhani wanaleta sadaka ya wanyama vipofu, wanaoumwa na wenye vilema. Ni muhimu kwetu kuleta sadaka kamilifu kwa Mungu wetu. Tunawaheshimu wazazi wetu, mabosi wetu, kwa nini Yeye tumletee vitu chakavu au visivyopendeza? Hata nasi leo hatupaswi kumletea BWANA vitu ambavyo havina maana. Tunajipatia laana, Naye atakemea mashamba yetu ili mbegu zisizae. BWANA anasema kuwa imepasa midomo ya watumishi wa Mungu iwe na maarifa, wasigeuke na kuacha njia na kuwakwaza washiriki wa kawaida kwa kutenda dhambi. Tukifanya yale yasiyopendeza, mbele za BWANA tutakuwa watu wa kudharauliwa.

Wayahudi waliambiwa kuwa wamesahau agano, ndiyo maana maombi yao hayakusikilizwa. Wanandoa walifanyiana hiana. Mungu anasema anachukia mume na mke kuachana au talaka, ni kutotunza ahadi. Mume na mke wakae siku zote katika furaha au kwa huzuni, bila kuachana. Ndoa iwe mbingu ndogo.

BWANA anaahidi kutuma mjumbe Wake, Naye ataitengeneza njia yake. “Lakini ni nani atakayestahimili siku ya kuja Kwake?…kwa maana Yeye ni mfano wa moto wa mtu asafishaye fedha, ni mfano wa sabuni ya mtu afuaye nguo.” Mungu anasema atakuwa shahidi kwa watendao uovu kama wachawi, wale waoneao wajane au yatima, wazinzi, waongo, wampotoshaye mgeni asipate haki yake. BWANA anasema kwa sababu hana kigeugeu ndio maana watu Wake hawakuangamizwa..

Mungu aliwaambia kuhusu zaka na sadaka ambazo hawakuwa wanatoa kwa uaminifu. Zaka ni moja ya kumi ya mali tunayopata mfano, tukipata shilingi kumi tunatoa moja, au tukipata machungwa ishirini, tunatoa mawili. Sadaka ni kile tunachotoa baada ya kutoa zaka. Zaka na sadaka hutumika katika kazi ya BWANA katika kueneza injili. Hebu tujifunze kutoa bila kunung’unika. Hatuwezi kupenda bila kutoa. Mungu anasema kwamba atawafungulia waaminifu madirisha ya mbinguni hata nafasi ya kuweka baraka isitoshe kwa kuwa watakuwa wamebarikiwa mno, na wanyama waharibifu hawataharibu mashamba yao. Mungu Mwenyewe atasimamia na kuhakikisha hawapungukiwi wala kuonewa. Niligundua kwamba nyumba tunayoishi ina madirisha 26 na milango mitatu, kumbe ndiyo maana tunaambiwa Mungu atafungua madirisha ya mbinguni na si milango, yaani baraka zitakuwa nyingi zaidi!

KWANINI turudishe Zaka?

1. Kwa sababu Mungu Amesema
2. ZAKA ni ya Mungu, na ni takatifu-Walawi 27:30
3. Kusapoti watenda kazi wa Injili- Hesabu 18:21 na 1Kor 9:13
4. Inaondoa uchoyo na ubinafsi 2 Wakor 9:7
5. Inakuza kumtumaini na kumtegemea Mungu
6. Ahadi za Baraka za Mungu Malaki 3:10
7. Inaonesha Yule tunayemtumikia kama ni Bwana au mali Luke 16:13

Wengine wakati wa Malaki walisema kwamba kumtumikia Mungu hakuna faida. Kwamba watu wabaya, na wenye kiburi ndio wanaopata raha. Lakini watu wamchao

BWANA walisemezana, Naye akasikia, akaandika majina yao katika kitabu cha kumbukumbu. Neno la Mungu linatuonesha kuwa kuna vitabu Vyake anavyoandika mambo yetu yote kule mbinguni. Hakika kila mtu anafurahi akisikia atafunguliwa madirisha ya mbinguni maana baraka zitakuwa tele, kawaida milango kwenye nyumba huwa ni michache kulinganisha na madirisha.

Je, nawe ungependa kuandikwa katika kitabu cha uzima? Kuwa kwenye kitabu hiki ni kitu cha thamani mno kupita vitu vyote unavyofikiri ni vizuri. Ni habari njema sana, maana Mungu ana zawadi kubwa na za ajabu zinazopita kifani kwa wote walioandikwa katika kitabu hiki. Kristo atakuja na kulisafisha hekalu. Kisha anasema kwamba jua la haki litawazukia wale wanaompenda Mungu, Jua la haki ni Kristo.

Kitabu cha Malaki kinamalizia kwa ujumbe kwamba BWANA atamtuma nabii Eliya ambaye "ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana."

Tujue kwamba tukilenga mbinguni, tutapata mbingu na mema ya dunia pia, ila tukilenga dunia tu, tutakosa mema ya dunia na kukosa kabisa yale ya mbinguni. Siku zote Jina Lake Bwana litakuwa kuu kati ya mataifa, kuanzia macheo ya jua mpaka machweo.

*Ikiwa hauhisi hatari yoyote, na ikiwa haufanyi maombi ya msaada na nguvu ya kupinga vishawishi, hakika utapotea; kupuuza kwako wajibu kutaandikwa katika kitabu cha MUNGU mbinguni, na utakutwa umepunguka katika siku ile mbaya ya hukumu.

Makuhani walikuwa na shida gani? Zaka ni nini? Kwa nini ni muhimu kutoa zaka? Kwa nini ni vibaya kutoa talaka? Kwa nini ni vibaya kuleta sadaka isiyo kamilifu au kilema kwa Mungu, mfalme wa dunia? Kama wangepeleka sadaka kilema kwa mtawala, ni nini kingetokea? Nabii Eliya alikusudiwa kufanya nini?

# AGANO JIPYA

## BAADA YA YESU AU MASIHI ISA BIN MARIAMU KUZALIWA

Agano la Kale ndilo gombo la kwanza la Biblia, waisraeli waliliita Tanak, yaani (a)Torati ikiwa ina maana mafundisho, (b) neviim/manabii na (c) Ketuvim (Maandiko)
1. Lugha- Agano la kale liliandikwa kwa Kiebrania. ila kitabu kama cha Daniel na Ezra viliandikwa Kiarameiki kwenye sura fulani. Agano Jipya lililandikwa Kigiriki.
2. Vitabu vya Biblia havijaandikiwa kutokana na muda wa matukio (Kronolojiko), ila matukio ya Agano Jipya yalikuwa baada ya Agano la Kale. Agano la Kale ni theluthi mbili, na Agano Jipya ni theluthi moja ya Biblia. Agano la Kale lina sura 929 na Agano Jipya lina sura 260. Agano Jipya ni Mwendelezo wa Agano la Kale, Maagano hayo mawili yanakamilishana! Yaani ni mwendelezo wa Jingine! Biblia ni barua ya upendo kutoka kwa Mungu kuja kwetu ambayo ina Neno Lake na ahadi Zake kwetu. Agano la Kale linazungumzia kuhusu kafara ya wanyama, wakati Agano Jipya linajikita kwenye maisha na mafundisho ya Yesu, na hatimaye Kifo Chake Msalabani.


Biblia ni ujumbe na chombo cha Mungu ili tumjue Mungu zaidi na kuimarisha imani yetu. Biblia ni barua ya upendo kutoka kwa Mungu kwetu ambayo ina Neno Lake na ahadi Zake kwetu. Kando na kusikia kutoka kwa Mungu, pia tunapata kuchungulia maisha mbalimbali ya wale walioishi katika zama tofauti. Tunajifunza kuhusu utamaduni wao, historia, na jinsi Mungu alivyofanya kazi katika maisha yao. Kwenye maisha haya kuna uwezekano mkubwa kuwa kuna mafumbo ya kina ambayo kwa sasa tunangojea yaweze kufunuliwa kwetu. Neno la Mungu hutusaidia kujenga imani yetu na kuimarisha uhusiano wetu wa kibinafsi na Yeye. Hebu Tunapoyagundua mafumbo au siri hizi zaidi, Biblia na iendelee kuwasha moto wa kiroho ndani ya mioyo yetu, kulishikilia Neno Lake mara zote. Kwa Jina la YESU KRISTO. Amina

*Maombi Sio Ushahidi wa Kuongoka Ikiwa Maisha Hayajabadilishwa—Shetani huwaongoza watu kufikiri kwamba kwa sababu wamehisi unyakuo wa hisia, basi wao wameongoka. Lakini uzoefu wao haujabadilika. Matendo yao ni sawa na hapo awali. Maisha yao hayaonyeshi matunda mazuri. Wanaomba mara kwa mara na kwa muda mrefu, na daima wanarejelea hisia walizokuwa nazo wakati fulani. Lakini hawaishi maisha mapya. Hawa wamedanganyika. Uzoefu wao hauzami ndani zaidi kuliko hisia zao. Wanajenga juu ya mchanga, na upepo mkali unapokuja, nyumba yao inafagiliwa mbali.

YESU abadilisha historia ya dunia, Kabla ya Kristo (KK) yawa Baada ya Kristo (KK)!

**SIKU YA 189**
**(Julai 7)**

# Je, Mungu ametusahau? Watu walijiuliza



Baada ya uumbaji na dhambi kuingia, watu walizaana na kutawanyika mbali na familia au koo zao. Wengine hawakuwa waaminifu kuwaambia watoto wao kuhusu Mwenyezi Mungu wa mbinguni, na hivyo Neno la Mungu likapotea, na hata ufahamu, maarifa na elimu ya kumjua Mungu wa Kweli aliyeumba mbingu na nchi yakapotea. Watu wakaanza kuabudu miungu mingine ya vitu vya duniani, mbinguni au majini. Watoto waliozaliwa hapo wakaanza kujiuliza maswali kama "Nani ameumba dunia? Nani ameumba miti, matunda, wanyama na maua? Au nani ameniumba mimi?"

Mungu anajifunua kwa kila mtu jinsi Yeye alivyo, kwani si mchoyo na si dhalimu. Watu wengi wamemwomba Mungu ajionyeshe kwao na akajionyesha. Hili ni ombi ambalo Mungu hawezi kuacha kulijibu. Ukiomba "BWANA nataka kukujua, kukufuata na kukutii." Yeye ni dhahiri atakujibu. Watu wemegundua kwamba kuna Mungu aliyeumba kila kitu. Hata wale wasio na kitabu cha Biblia wanafahamu hilo. Mungu amejionyesha kwao kupitia viumbe vya asili, jua, mwezi nyota wanyama samaki ndege na kadhalika. Mungu amejifunua kupitia katika Neno Lake yaani Biblia, na zaidi ya hayo amejifunua kupitia katika Yesu Kristo aliyeacha mbingu na kushuka katika ulimwengu huu. Kwa vile mafunuo Yake ya wazi zaidi yako kupitia Biblia, na Biblia inaweza kupatikana katika maduka mengi ya vitabu vya dini ni vizuri kila mmoja afanye bidii ya kupata kitabu hiki cha pekee.

Mama mmoja kule Kateshi Tanzania alitusimulia kisa cha ajabu. Huyu mama alitaka sana kujua Neno la Mungu, na Mungu alimfunulia njia. Kila mtu alipotoa udhuru

wa kumfundisha kwa madai kuwa ana shughuli, asiweze kumfundisha, muujiza ulitokea. Siku moja asubuhi, alichukua kitabu cha Neno la Mungu, akafungua kitabu cha Mathayo katika mahubiri ya mlimani au 'Mlima wa Baraka, huku akiwa anaenda machungani. Alipofika kule alikifungua kitabu, na akaweza kukisoma bila ya kufundishwa na mtu yeyote. Hii ilikuwa zawadi yake toka mbinguni. Toka siku ile aliweza kusoma Neno la Mungu bila shida.

Mwenyezi Mungu ana uwezo wote, ni mtoaji wa yote mema, na anajibu maombi ya watu, na hasa ya watoto! Mjaribu leo, ukamwambie wataka kumjua na kumtumikia, atakujibu kuzidi vile shauku yako inavyotegemea na kuzidi watu wanavyofikiria. Haijaanguka ahadi yake hata moja, kati ya zile ahadi 3,500+ alizoahidi, amezitimiza na hata kuzidi. Mwenyezi Mungu ana nguvu zote na pia aweza kumwamsha mtoto mvivu, mnyonge, au mwenye usingizi asome Neno Lake. Amekupa uchaguzi wa kusoma Neno Lake, hakuamrishi. Kama una muda wa kula chakula, basi una muda wa kula Neno Lake! Ukiona hauna muda, sema sitakula chakula mpaka nile Neno, nawe utaona ombi lako likijibiwa mara moja!

Watu walipoanza kuabudu Miungu mingine, Mungu alijitokeza kwa Nuhu, kisha Ibrahimu, akamwambia ahamie Kanani. Akamwambia uzao wake watakuwa watu maalumu. Uzao wa Ibrahimu ukaenda Misri wakati wa njaa kubwa na kukaa kule miaka 430. Baadaye wakawa watumwa na Mungu akawatoa kwenye shida hii kupitia mtoto aliyezaliwa na kuitwa Musa. Mungu aliwapenda WaIsraeli, na kupitia kwake alitaka kuonyesha uwezo, upendo, haki na rehema Zake kwetu sisi wote, yaani dunia nzima. Musa alitii, Waisraeli wakaona ukuu wa Mungu na msaada wake tena na tena. Walipolishwa, kuvishwa, kulindwa na kufanyiwa makuu yote waligundua tena kwamba kuna Mungu.

Ubaya ni kwamba Waisraeli walisahau tena na walipotumiwa manabii tena na tena hawakutaka kusikia maagizo ya BWANA. Basi walitekwa na Wakaldayo na kwenda kuishi Babeli miaka 70. Mwishowe walirudi kwao, na makuhani na waandishi wakawasaidia tena kuanza kusoma Maandiko Matakatifu na kumjua Mungu na tabia yake halisi. Sheria zake ni kwa ajili yetu. Zimejaa upendo na si za kutukosesha raha. Je unapenda kuwa na jirani asiyeshika sheria au mwovu? Sidhani, maana, uko hatarini kufanyiwa ovu lolote. Muhtasari wa sheria ni mpende BWANA Mungu wako kwa moyo, akili, nguvu, na roho yako yote na jirani kama nafsi yako.

Wengi hufikiri ni bora kujiamini wenyewe kuliko kumwamini Mungu. Watu hufikiri wanajua wenyewe chema na kibaya, hata zaidi ya Mungu. Mungu ni mwumbaji na anajua mno kile chema na cha kutupa furaha kuliko sisi. Kwani anatupenda kuliko sisi tunavyojipenda wenyewe. Na wale tunaowapenda Yeye anawapenda zaidi, na kuwatakia mema zaidi ya sisi. Dhambi inatupa huzuni. Japo Mungu alimwumba Adamu na Hawa kuishi milele dhambi yaani kutotii, iliwaletea huzuni nyingi; hata waliona mtoto wao wa kwanza akimwua mtoto wao wa pili.

Binadamu wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Mungu hakutaka sisi watoto wake tupotee milele, hivyo alifanya mpango wa wokovu wetu kupitia Mwana Wake Yesu aje duniani na kuishi bila dhambi na kufa, ili tuone tabia

ya Mungu ilivyo. Katika Agano la Kale kifo Chake Yesu, kiliwakilishwa na sadaka za kuteketezwa za wanakondoo au wanyama. Wanyama walikufa badala ya mtu aliyefanya dhambi. Wanyama walikuwa mfano tu, ili tupate picha ya jinsi dhambi inavyoweza kuondolewa. Yesu Ndiye alichukua dhambi zetu na kubeba madhaifu yetu. Kristo alichagua kufa kwa ajili ya dhambi zetu ili tusife milele.

Kristo alifanya tusiwe na utenganisho na Mungu. Huu ndiyo ulikuwa mpango wa Mungu wa wokovu kwetu sote. Wanyama waliokufa walimwakilisha Kristo. Pengine leo kwa kuwa hatutoi kafara ya mbuzi na ng'ombe maana Yesu alitufia basi tunakosa kuelewa jambo hilo vizuri. Hata hivyo tukimruhusu, Mungu atatupa mwanga wa Neno hili, maana Yeye ni "Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Watu wa zamani kafara iliwagharimu pesa, na wengine wasiojua waliichukulia kama jambo la kujipatia faida ya kiuchumi.

Na mbaya zaidi baada ya muda makuhani na watu walisahau kwamba kafara za hawa wanyama ilikuwa tu mfano wa kafara ya Yesu. Wakajiwekea sheria nyingi na kutaka watu wazishike ili wapate 'kuokolewa'. Wakafikiri watajitafutia uzima wa milele au wokovu wenyewe kwa kujishughulisha kwa nguvu nyingi. Wengine wakaingia tamaa ya uchumi, ikawa biashara na kipato cha kulangua mifugo. Wakasahau kuokolewa au uzima wa milele ni zawadi na Neema kwa kumwamini tu Mungu, na siyo kwa kujishughulisha na sheria. Kile cha muhimu tunachopaswa kufanya leo ni kuamini Yesu alikuja, akaishi na watu, na kisha akafa kwa ajili ya dhambi zetu, na Kisha akafufuka. Cha muhimu sasa ni kuipokea karama au zawadi hii.

Hata leo wengi hawaelewi upendo huu mkuu wa Mungu. Wanafikiri Mungu ni katili, asiyependa urafiki ambaye shughuli Zake kila mara ni kuangalia 'ni nani amefanya makosa' ili amkamate na kumtwanga. Huu ni uongo ambao Ibilisi ameweka vichwani mwetu. Mungu ni upendo, anatupenda na kutaka kutupa furaha ya kweli. Mungu alimtuma mwanawe ili tuingize jambo hili mawazoni mwetu ili tuepuke huzuni zinazoletwa na dhambi. Tafuta kitabu kinaitwa Njia salama, usome sura ya Kwanza, kuhusu upendo wa Mungu kwa mwanadamu! Dunia ilimngoja Masihi au Mwana-Kondoo wa kweli azichukuaye dhambi za ulimwengu, na muda ukawadia. Mungu daima hutunza ahadi Zake. Mungu alipomtuma Mwana Wake, Wayahudi hawakuwa huru bali chini ya Warumi. Warumi walimweka Herodi kuwa mfalme wa sehemu hiyo. Japo Herodi aliwajengea au alikarabati hekalu lao mwaka wa 20BK, walimwogopa Herodi sana kwa ukatili wake, na kisha wakawaogopa Warumi waliowatawala. Warumi wangechukua koti la mtu au wangemwambia mtu awabebe mizigo na mtu asipinge.

Siku zile Wayahudi walijiuliza "Je Mungu ametusahau? Kwa nini tuna maisha magumu hivi?" Walikuwa wameshatolewa kwenye utumwa wa Misri, na ule wa Babeli na Mungu mwenyewe. Sasa wakaona huu utumwa wa Warumi uliobaki Mungu ataushugulikia na kuwaondolea nao mbali. Wayahudi waliposoma Maandiko wakajua Mkombozi atakuja na atamponda kichwa Shetani wakadhani pia atawafukuza Warumi na kufanya nchi yao iwe na nguvu na tajiri. Wengine walifikiri akizaliwa Masihi atawapa Paradiso au wataenda mbinguni papo hapo

bila ya Masihi kufa msalabani kwanza. Yesu alisisitiza kwamba imempasa kufa ili sisi binadamu tuokolewe. Hili Neno ya kuwa "LAZIMA KUFA' hawakulielewa, mpaka pale waliposhuhudia kwa macho yao akifa, na kufufuka na kisha kupaa. Wametuandikia waliyoyaona kwa macho yao, ili nasi kwa saburi na imani tupate wokovu. Manabii wengi kama Isaya, Daudi, Zakaria, Hosea waliandika kuhusu Masihi. Kuna zaidi ya unabii 125 wa Agano la Kale uliotimia kuhusu Masihi.

Profesa Peter Stoner, akiwa anafundisha Pasedina California, masomo ya sayansi, uhandisi na elimu ya anga alifanya mahesabu ya takwimu ya uwezekano (probability) wa unabii 8 utokee kwenye maisha ya mtu mmoja, alipata kuwa kuna uwezekano upatao 1 kwa 100,000,000,000,000,000,000,000,000,000. Kwa kujua zaidi Dr Sudhat Pandit aliyezaliwa wanapoabudu miungu mingi alifanyia utafiti kuona kama Dini ya Kikristo ina uhakika nje ya Biblia na kama ina uwezo wa kubadilisha maisha ya watu. Akakuta shuhuda nyingi, kama zaidi ya unabii 600 wa Biblia uliotimia. Angalia tovuti yake ya Comeandsearchwithme.com

*Mtafute Bwana kwa Moyo Wote — Maombi yetu yanapaswa kujazwa na upole, huruma na upendo. Tunapotamani ufahamu wa kina na mpana zaidi wa upendo wa Mwokozi, tutamlilia MUNGU atupatie hekima zaidi. Ikiwa kulikuwa na haja ya sala na mahubiri yanayochochea roho, ni sasa. Mwisho wa vitu vyote umekaribia. Laiti tungeweza kuona kama tunavyotakiwa, umuhimu wa kumtafuta Bwana kwa moyo wote! Basi Tungelimpata. Hebu MUNGU na awafundishe watu Wake jinsi ya kuomba.


-------------------------------

Maswali: Je umemwomba Mungu ajionyeshe kwako? Kuna ahadi ngapi za Biblia? Unabii wa Agano la Kale kuhusu Masihi umetimia kwa kiasi gani? Kafara watu walizotoa kabla ya Yesu kuja zilikuwa na maana gani? Kwa nini kujua kusoma ni muhimu kwa mtu anayempenda Mungu? Kwa nini ilikuwa LAZIMA Yesu afe? Je twajuaje leo kama watu wa zamani tunaosimuliwa habari zao waliishi au walikuwako kweli? (mfano Ibini Batuta, Mansa Musa, Vasco da Gama, Mfalme Henry wa Uingereza, Askia mkuu au George Washington).

**SIKU YA 190.**
**(Julai 8)**

# Vitabu vinne vya injili.

**Mathayo, Marko, Luka na Yohana.**



Vitabu vinne vimeandika kuhusu maisha ya Yesu, kufa Kwake, kufufuka na kupaa Kwake mbinguni. Hivi vyaitwa vitabu vya injili. Mathayo ndicho cha kwanza, ila Marko ndiye aliyeandika kabla ya wote. Hawa wanazungumzia yaliyotokea kipindi cha 4BK mpaka 30BK. Vitabu hivi vinatusaidia tupate picha kamilifu ya kuzaliwa, kuhudumu, kufa na kufufuka kwa Yesu. Barua za Paulo kama Wagalatia na Wathesalonike ziliandikwa kabla ya vitabu vya injili. Mathayo alikuwa mtume au mwanafunzi wa Yesu, na jina lake jingine lilikuwa Lawi. Kabla ya utume alikuwa mtoza ushuru. Yeye aliwaandikia watu akiwaelezea habari njema za Yesu aliyekuja wakati ulipotimia. Masihi hakuwahi wala hakuchelewa kuzaliwa. Alitaka kutuhakikishia wote tutakaosoma, na hasa Wayahudi kwamba Yesu ni Masihi aliyeahidiwa kwenye Agano la Kale.

Injili ni habari njema za kuzaliwa kwa Yesu, maisha Yake, mafundisho Yake, kifo Zake na kufufuka Kwake. Hiki ni kisa cha mpango wa wokovu, yaani wokovu wetu wanadamu. Mathayo aliandika mafundisho mengi ya Yesu, akasisitiza unabii wa Agano la Kale uliotimia kuhusu Masihi, zaidi ya mara 27. Injili ya Mathayo ndiyo inasomwa na kunukuliwa na wengi zaidi. Pengine hiyo ndiyo sababu ikatangulia kuwekwa mwanzo wa Agano Jipya. Mathayo ina maana zawadi ya Mungu. Mathayo anaanza kutuelezea historia ya ukoo wa Yesu Kristo akianzia Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Yuda…Boazi, Obedi, Yese, Daudi, Sulemani….Zerubabeli…Yusufu

mumewe Mariamu na kisha Yesu mwenyewe.

Anatujulisha kuwa vizazi vyote toka Ibrahimu mpaka Daudi ni 14, na Daudi mpaka uhamisho wa Babeli 14, na tangu ule uhamisho wa Babeli mpaka Kristo kuzaliwa ni 14, jumla 42. Luka anaelezea ukoo wa Yesu akirudi nyuma mpaka kwa Adamu "akidhaniwa Mwana wa Yusufu, wa Eli, wa Mathati, wa Lawi…. … wa Adamu, wa Mungu." Ukoo wa Yesu watuonyesha Mungu ana waaminifu wanaomfuata kwenye kila kizazi, taifa na jamaa. Wayahudi walijaribu kuwafanya wengine wasiingie dini yao. Ila Yesu alipokuja aliwaita watu wa aina zote au wa mataifa yote, wamfuate.
Marko au Yohana Marko ndiye aliyeandika kitabu cha Injili cha kwanza. Kitabu hiki ni kifupi, na kiko wazi na chenye matukio mengi. Yeye alianzia maisha ya kuanza kazi kwa Yesu ukubwani. Alitaka watu wamwamini Yesu mwana wa Mungu na Mwana Adamu, ili wapate wokovu. Mwana Adamu imeandikwa mara 93 kwenye Agano Jipya. Yaonekana Ezekieli naye alipokuwa kuhani aliitwa jina hili mara 93, nabii huyu alimwakilisha Mungu kwa watu wa Babeli.

Marko alisimuliwa habari za Yesu na Petro, aliyekuwa mtume, au mwanafunzi wa Kristo. Alikuwa akifanya kazi chini ya Petro kama mwana wake katika Kristo (1 Petro 5:13). Kristo ni Neno la Kiyunani likimaanisha Mpakwa mafuta au Masihi. Marko alikuwa kijana wa Mariamu na mpwa wa Baranabasi mwana wa matumaini, mhubiri wa kutoka Antiokia, Syria. Marko aliandika kwa wauumini wa mataifa kama Warumi. Anakazia matendo makuu ya Yesu, zaidi ya mafundisho ya Yesu na kwamba ni Mtumishi wa Mungu atakayeteswa na kuwa kafara kwa ajili yetu; na ndiyo maana anaeleza miujiza 27.

Tabibu mpendwa Luka ameandika kitabu cha tatu cha injili kwa Theofilo, ambaye ni kiongozi wa Kirumi. Luka alikuwa mtu wa mataifa, yaani hakuwa Myahudi bali Myunani. Yeye ni mwanasayansi aliyefanya uchunguzi au utafiti, akihoji watu, waliomjua na kumhudumia Yesu. Amekazia mifano ya Yesu kama 19 hivi kati ya 29 iliyorekodiwa. Mifano hii ni vile visa vya kawaida vya duniani, Yesu alivyosimulia ili kuleta mafundisho ya kiroho au ya mbinguni kwa mambo ya kawaida au ya kila siku maishani mwetu. Mfano wa mifano hiyo ni mwana mpotevu, mpandaji mbegu (mpanzi), Msamaria mwema na vinginevyo.

Luka alitembea na Paulo katika safari zake tatu za umishonari, na akaandika kitabu cha Matendo ya mitume pia. Safari yao ya mwisho na Paulo iliwapeleka Rumi kwenye merikebu iliyovunjika, bali wote 276 wakasalimika. Paulo alimshuhudia Yesu miji waliyopita, na hatimaye katika mji wa Rumi. Luka anakazia Yesu kama "mwana wa Adamu" mara 80. Aliandika ili wasomaji wajue kweli, kuhusu maisha ya Yesu kama Mkombozi wa dunia, mponyaji na mfariji. Luka kama tabibu ana huruma na anakazia huduma ya kuponya wagonjwa, kusaidia masikini na waliotengwa. Luka anajulikana kama tabibu aliyependwa. Watalaamu wampendao Mungu na wasiompenda wa vitabu vya Kale wamehakikisha kwamba kitabu cha Luka ndicho cha kwanza kwa uhakika. Hii ni kwa vile walienda kuona nchi 34 aliyoisema na wakakuta ni ya uhakika.

Yohana mpendwa, ameandika kitabu chake tofauti kidogo na zile injili zingine. Yeye anakazia mafundisho ya kiroho ya Yesu zaidi ya masimulizi ya yaliyotokea au historia. Ukisoma kuanzia Yohana 1, 8 au 13-17 utaelewa vizuri, maana ni yeye tu ameandika mafundisho haya. Yohana anaanza maisha ya Yesu mbinguni na nyuma kabla ya hapo. Anazungumzia milele zote za nyuma na mbele. Yohana alikuwa mwanafunzi au mtume wa Yesu ambaye ndiye alikuwa mdogo kwa umri. Aliishi mpaka miaka zaidi ya 90, akaandika kitabu cha Ufunuo, na barua tatu kwa makanisa. Huyu mtume mara zingine anaitwa mtume wa upendo. Amekazia sana upendo hata kwenye nyaraka zake ameandika "Mungu ni upendo" au "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe…."

Yohana aliwaandikia Wayahudi ili wajue Yesu ni Mwana wa Mungu anayeichukua dhambi ya ulimwengu, na kwa kujua hivyo, waokoke. Yohana haanzi kitabu cha injili kwa kuelezea ukoo wa Yesu, anarudi chanzo halisi cha Yesu, yaani umilele Wake na Uungu Wake. Anamtambulisha Yesu kama Neno, aliyeumba mbingu na nchi, na Yesu kama Mungu. "Hapo mwanzo kulikuwako na Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo, wala pasipo Yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. Nayo nuru ya kung'aa gizani, wala giza halikuiweza."

Kuwa Mkristo ni pamoja na kuamini Yesu ni Mungu. Hii ndiyo imani yetu Wakristo, tunaamini kwamba Yesu ni Mungu, na ndiyo maana malaika alisema ataitwa 'Emanueli, maana yake Mungu pamoja nasi.' "Malaika akawambia wachungaji, msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi Ndiye Kristo, BWANA."

Neno hili BWANA ndiyo lile linalotumika kwa Mungu kwenye Agano la Kale, Mungu alipotajwa. Uungu ni fumbo, na siri ambayo kwetu sisi binadamu hatuwezi kuelewa kwa ndani. Hata malaika, walipoona Muumbaji wao akichagua sayari yenye giza, ndogo na chafu chafu, eti aende azaliwe pale na kutembea na kufanya vitu kama sisi binadamu tuliozidiwa, walishangaa sana. Inakuwaje MUNGU wao Mkuu, ajishushe kiasi hicho? Basi sisi wakazi wa dunia, tuwe na furaha, na kuchangamka, tuinue macho yetu juu, maana tumekirimiwa sana kuwa ile sayari iliyochaguliwa na Muumba, aliyopanga tangu milele aje na kutufia.

Hebu tushangilie leo, kwa kuokolewa. Katika dini zote kubwa hakuna kiongozi aliyedai ni Mungu au mwana wa Mungu. Yesu tu Ndiye aliyedai, Naye pekee tu ndiye ameweza kuandikwa na waanzilishi wa madhehebu mengine kama Uislamu, na dini ya Kiyahudi. Maandiko ya dini nyingi yametaja habari zake kwa uchache mfano Budha ni mara 10 tu. Kupatikana kwa Maandiko mengi yasiyobadilishwa kwadhihirisha Ukweli na uthabiti Wake. Maandiko ya Biblia ya Kiyunani, Kiebrania na Kiaramaiki yamepatikana yapatayo 5664 na ukijumlisha lugha zote Agano Jipya limenakiliwa kwenye vitabu vya Kiarabu mara takribani 30,000. Hili linadhihirisha kwamba Biblia ni ya uhakika, maana yakiwa mengi na hayatofautiani, basi ni ya kweli.


*Maombi Sio upotezaji wa muda - Kila asubuhi chukua muda kuanza kazi yako na sala. Usifikirie kuwa kufanya hivi ni upotezaji wa mida; huu ni wakati ambao utaishi milele zote (enzi zote). Kwa njia hii mafanikio na ushindi wa kiroho yataletwa. Mwili wako utaitikia mguso wa Mkono wa Mwalimu na Bwana. Hakika baraka za MUNGU zinastahili na kufaa kuombwa, na kazi haiwezi kufanywa kwa usahihi isipokuwa ina mwanzo unaofaa. Mikono ya kila mfanyakazi lazima iimarishwe, moyo wake lazima utakaswe, kabla Bwana hajamtumia kwa ufanisi zaidi.

---

Maswali: Injili maana yake nini? Watu gani wanne waliandika vitabu vya injili? Je? waweza kusema tofauti zao? Je, kila mwandishi wa injili aliandika kwa nani na kwa madhumuni gani? Je Mathayo, Luka na Yohana walifanya kazi gani kabla ya kuandika injili? Je tunajuaje kwamba Yesu ni BWANA au Mungu? Je Mtu akikuuliza Kwa nini wewe unamwamini Yesu, waweza kumwelezea, mambo ya uhakika, nje ya Biblia yako? Kama la! hima anza kufanya utafiti wako binafsi, usiwe mtu wa kuigiza tu!

**SIKU YA 191.**
**(Julai 9)**

# YESU Alikuwako siku zote, na anaendelea kuishi milele.



Tulipoanza kuandika Biblia ya watoto sehemu hii ya Agano Jipya, niliona tumepungua sana, na kwamba Kisa hiki cha thamani tutakisimuliaje maskini, maana maneno ya kibinadamu hayatoshi, na uzoefu wetu ni mdogo mno. Tunapoandika maisha ya Yesu, tunashindwa tuanzie wapi. Twaweza kuanzia Bethlehemu, ila hii itakuwa imepungua au kukosekana maana halisi inayojitosheleza. Maana Bethlehemu, inaonyesha miaka yake 33 tu ya hapa duniani, kati ya miaka yake isiyo mwanzo wala mwisho. Maana maisha ya Yesu hayana mwanzo wala mwisho ni milele alikotokea nyuma milele na siku zinazokuja milele!

Kisa Chake hapa kinaanzia kwenye kufanyika Kwake mwili, alivyofanya huduma Yake duniani na alivyokwenda mbinguni kuendelea na umilele. Natumia Maneno haya, maana lugha ya Kiswahili haijayaazima bado kutoka kwenye lugha za zamani. Kingereza kimeazima mengi. Tukisoma Luka 2:10,11 malaika anawaambia wachungaji wasiogope kwani ameleta habari njema zenye furaha "Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa kwa ajili yenu, Mwokozi ndiye Kristo BWANA." Kama

tulivyokwisha kuona, cha ajabu kupita yote hapa inasema mtoto huyu mchanga ni “Kristo BWANA.” BWANA ni Neno ambalo Wayunani walitumia badala ya YAHWEH, Jina la Mungu ambalo limetumika kwenye Agano la Kale. Hivyo malaika alisema kwa wazi kwamba mtoto yule ni Mungu.

Jina Masihi pia lina maana ya Uungu wa Yesu. Habari njema za malaika zaendelea kusema kwamba atakuwa Mkombozi wa dunia yote. Hebu mimi na wewe tushangilie na kupiga vigelegele pamoja na malaika kwa ukombozi wetu. Najua hatutakuwa tumefanya haki kuelezea maisha yake, ila tutajaribu kidogo kwa vile haiwezekani kwa binadamu kusimulia kisa hiki, kwani kinatuzidi maarifa na upeo wetu wa kibinadamu. Kila baba anakuwa na woga wa kumwachia mtoto wake kwa watu waovu au wenye hatari, anapenda kumlinda mtoto wake. Mungu Yeye alimtuma Mwana Wake wa pekee kwenye dunia ya hatari, kuhatarisha maisha Yake ili watoto wetu wawe na usalama wa milele siku moja.

Yohana anatuambia wazi anapoanza Yohana moja “Hapo mwanzo kulikuwa na Neno, na Neno alikuwa na Mungu, na Neno alikuwa Mungu.” Hii yaendana na “Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi” Mwanzo 1:1. Yohana mtume anatuchukua mwanzo wa Kisa cha Yesu, na mtume Paulo anamalizia katika Wakolosai “Kwa kuwa katika Yeye vitu vyote viliumbwa vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi; vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia Yake na kwa jili Yake.” Yesu mwanzo Wake haukuwa katika uumbaji bali milele zote, kwani mawazo ya binadamu ambayo yana muda, maada na kuchukua nafasi, inakuwa vigumu kuelewa siri au fumbo hili.

Tungetamani Mungu aweze kuelezewa au kueleweka katika lugha yetu au mahitaji Yake yafanane na yetu!. “Vitu vyote viliumbwa kupitia Yeye, na bila Yeye hakuna kilichoumbwa.” Isaya naye anaongezea “Tumepewa mtoto mwanamume…Naye ataitwa mshauri wa ajabu, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi Yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe… tangu sasa na hata milele.” Jaribu kumtafuta YESU kwenye Agano la Kale, maana huko amejaa! Yule Mimi Niko, Ni Yeye!

Wayahudi walishtuka waliposikia Yesu akisema “Amini Amini nawaambia yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Wayahudi walifikiri kwamba huyu ‘asiye na miaka 50 atakuwaje miaka maelfu iliyopita amwone Abrahamu, kama si Mungu’. Basi wakataka kumpiga mawe maana walikumbuka “MIMI NIKO” ni jina lingine la Mungu ambalo Musa aliambiwa kwenye Kutoka 3. Mtume Paulo na wengi wamesema “wameazimia wasijue neno lolote, isipokuwa Yesu Kristo Yeye aliyesulubishwa.” Sisi nawe pia liwe ombi letu leo, ‘Tusiazimie kujua neno lingine isipokuwa Yesu aliyesulubishwa’. Manabii, mitume na waanzilishi wa dini zote wamelala wakingoja ufufuo, Ila Yesu ni mzima yuko hai mbinguni katika kiti cha enzi, mkono wa kuume wa Mwenyezi Mungu. Watu 500 walishuhudia akipaa bila ndege, baada ya kuwa nao kwa siku 40!

Kuna wimbo unasema "Tugeuze macho yetu na tumtazame Yesu tuangalie upendo Wake wa ajabu, mambo ya dunia hugeuka, na kuchuja, uso Wake Yesu tukiuona." YESU hachuji kamwe. Katika Agano Jipya tutamtazame Yesu kwa makini maana Ndiye Alfa na Omega Mwanzo na Mwisho. Kitu kikubwa ni kwamba Mungu anataka kuwa rafiki yetu, kila mmoja wetu, anataka tuzungumze naye na kumwambia yanayoendelea kwetu, iwe ni ya furaha, huzuni, au mambo ya kawaida. Anatupenda na kutaka kutupa furaha. Anataka kutusaidia na ndiyo maana akamtuma Mwanawe. Yote yanapita, ila Yeye ni wa milele, na anataka tuwe Naye milele. Tumkaribishe mioyoni mwetu.

Muda mwingi WaIsraeli walimngoja Yesu. Bali wengine walianza kusahau, kwamba zile kafara wanazotoa zinamwakilisha Masihi atakayekuja na kufa kwa ajili yao. Kafara ikawa mapokeo au shughuli ya kawaida inayofanyika kwa lengo la kuwainua kiuchumi. Yesu alichagua kufa ili tusitengwe kamwe tena na Mungu. Uzima wa milele ni zawadi. Tunachopaswa kufanya ni kuamini tu, bila kutegemea akili au uwezo wetu. Tumtegemee Yeye tu! Tuamini alikuja kuishi duniani na kufa ili tupate uzima. Tumkiri kwa midomo yetu, mawazo yetu, nia zetu na kisha tuungame, na kuishi kwa mahusiano Naye, huu ndiyo uzima wa milele. Yeye atatusaidia kuwa watu wema, na siyo kutusaidia kutenda mema tu. Kutenda mema, na kuwa mwema kuna tofauti kubwa.

Tunashauriwa tuwe na nia kama ya Yesu ya unyenyekevu "Yeye aliyekuwa Mungu ila hakuona kama kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho. Bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa mfano wa mwanadamu." Basi iwe ni jambo zuri kwetu kutumia muda kila siku kutafakari kwa makini habari za Yesu Kristo mioyoni mwetu. Tukivuta usikivu hatua kwa hatua kuangalia picha halisi ya mlolongo wa tukio hili, hasa hili tunalohitimishia.

*Ushindi Kupitia Maombi ya Kila Siku — Kupitia maombi ya kila siku kwa MUNGU, watakuwa na hekima na neema kutoka Kwake ili kumudu mizozo na hali halisi ngumu za maisha, na kisha watatokeza kama washindi. Uadilifu na utulivu wa akili unaweza kuhifadhiwa kwa kukesha na kuomba tu.

---

Maswali: Yesu ana miaka mingapi leo hivi? Kwa nini Yesu alichagua kufa? MIMI NIKO ni Jina la Nani? Milele maana yake ni nini? Kumtazama Yesu kuna maana gani? Kwa nini tugeuze macho yetu kumtazama Yesu kila mara? Mtu akikuuliza umpe uhakika kwamba Yesu alikuja na kuishi duniani utamwambia sababu zipi za kibinadamu? Kwa nini malaika hawakuwatokea watu wenye kazi za wadhifa mkubwa? Kuna tofauti gani kuwa mwema, na kutenda mambo mema?

**SIKU YA 192.**
**(Julai 10)**

# Unabii wa kuzaliwa kwa Yesu Masihi na BWANA wetu.

**Luka 1.**



Wengi wanapenda mtoto azaliwe nyumbani mwao. Wanangoja kwa shauku kubwa, na shamra shamra. Yesu alikuwa amesubiriwa kwa maelfu ya miaka kabla ya kuzaliwa kama mwanadamu. Ahadi za Mungu zilisema atakuwa mtoto maalumu. Unabii kama ule wa Danieli 9 ulifunua zaidi wakati gani atazaliwa, yaani majuma 69 au siku (miaka) 483 kutoka mbiu ya kujenga Yerusalemu. Ila wengi hawakuwa wamesoma au kufunuliwa. Wasichana wengine, walifikiri pengine wao wangechaguliwa kuzaa mtoto huyu. Mtoto huyu aliahidiwa kutoka bustani ya Edeni baada ya dhambi ya kwanza kuingia.

Mungu aliahidi kuna siku Mtoto mwanamume atazaliwa Naye ataponda kichwa cha Nyoka au Shetani. Hawa alifikiri atazaa mtoto huyu, ila Kaini alipozaliwa hakuwa Yeye Yule Mkombozi, bali akawa mwuaji. Ikaendelea hivi kwa kila mzazi, wakipasiana ahadi waliyopewa, na huku wakiingojea. Zikapita karne na karne. Hata Musa aliwaambia watu Wake "BWANA Mungu wako atamwinua nabii kati yenu" Baalamu aliambiwa ahadi hii pia Naye akasema "itakuja Nyota" Isaya, Mika, Hagai, Zekaria na wengine, walitabiri pia.

Siku zilipokaribia, mbinguni kukawa na pilikapilika, kwani Mungu Mwana waliyempenda na kumwabudu malaika alikuwa tayari kuacha mbingu na utukufu

na akae katika sayari ndogo aliyoiumba, kuonyesha upendo Wake kwa viumbe Wake, japo walikuwa wamemwasi. Alikuwa anaenda kuchukua mwili wa binadamu na kuishi na binadamu. Hatujui kama malaika walielewa jambo hili vizuri, ila huu ulikuwa ushahidi mkubwa kwao kwamba Mungu ni upendo.

Malaika kwa shauku nao wakajitayarisha na kwaya ya mbinguni kuimba wimbo duniani wakati ule alipozaliwa. Yesu hakuchelewa wala hakuwahi. Wakati ulipowadia alizaliwa. Kwa nini Mariamu alichaguliwa hatujui, ila macho ya Mungu yalienda kila mahali na kuona wale walio wakamilifu Kwake. Hata wewe leo unayesoma, macho ya Mungu yanakuangalia, uwe mtoto au mkubwa. Mariamu alikuwa msichana, ndiyo tu alikuwa amemaliza utoto. Lazima Mariamu, alikuwa msichana wa pekee, Mungu alikuwa amemjua na kwamba moyo wake ni mkamilifu na kwamba anaweza kumpa tunu ya kumpa Mwana Wake wa Pekee.

Mungu alijua mtaa, nyumba na hata chumba Mariamu anakoishi. Akamtuma malaika Gabreli nyumbani kwa Mariamu kwenye mji wa Nazareti kwa bikira aliyekuwa ameposwa na Yusufu wa mbari ya Daudi. Malaika akaingia kwake Mariamu na kusema "Salamu, uliyepewa neema BWANA yu pamoja nawe." Mariamu akafadhaika sana, kwa ajili ya Maneno yale, akawaza moyoni, "salaam hii ina maana gani?" Malaika akasema "usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu. Tazama utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume, na Jina Lake utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu, ataitwa mwana wa Aliye juu, na BWANA Mungu atampa kiti cha enzi ya Daudi, Baba yake. Atamiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho. Mariamu akamwambia Malaika, litakuwaje Neno hili, maana sijui mume? Malaika akamwambia "Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu Zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu. Tena jamaa yako Elizabeti amechukua mimba ya mtoto mwanamume uzeeni, na mwezi huu ni wa sita kwake yeye aliyeitwa tasa, kwa kuwa kwa Mungu hakuna lisilowezekana." Mariamu akasema kwa unyenyekevu "Tazama, mimi ni mjakazi wa BWANA na iwe kwangu kama ulivyosema."

Malaika akaenda zake. Mariamu akawaza kwamba kuzaa ni jambo linalowezekana, lakini kuzaa bila kuwa na mume, ni jambo gumu, ambalo halijawahi kusikika. Mariamu hakungoja atumikiwe, ila akaenda mbali kilomita zaidi ya 100, katika nchi ya milimani kwa haraka mpaka mji mmoja wa Yuda kwa yule binamu yake Elizabeti ili amsaidie katika hali yake. Mariamu alikuwa wazi kumwambia yote binamu yake aliyekuwa mzee pengine wa rika la nyanya yake kwa ajili ya mahusiano waliyokuwa nayo. Ndipo akaingia nyumbani mwa Zakaria, aliyeoa binamu yake Elizabeti. Alipofika akamwamkia Elizabeti, ikawa Elizabeti aliposikia ile salaamu, ya Mariamu, hapo hapo kitoto kichanga kikaruka ndani ya tumbo lake.

Elizabeti akajazwa na Roho Mtakatifu, akapaza sauti kwa nguvu na kusema kwa Mariamu "umebarikiwa wewe katika wanawake, naye mzao wa tumbo lako amebarikiwa." Elizabeti akashangaa, limetokeaje neno hili, hata mama wa BWANA yaani Yesu amjie yeye. Akamwambia aliposikia sauti yake tu, mtoto, aliyekuwa ndani ya tumbo lake aliruka kwa shangwe. Elizabeti akasema heri aliyesadiki maana

yatatimizwa aliyoambiwa na BWANA. Mariamu akamsifu Mungu. Maneno hayo ya sifa kwa Mungu Walatini waliyaita 'magnifikati'. Wengi wamesema Maneno haya yamefanana kidogo na ya Hana mama wa Samweli na Miriam, dada wa Nabii Musa.

"Moyo wangu wamwadhimisha BWANA. Na roho yangu imemfurahia Mungu, Mwokozi wangu; Kwa kuwa ameutazama unyonge wa mjakazi wake. Kwa maana, tazama, tokea sasa vizazi vyote wataniita mbarikiwa. Kwa kuwa Mwenye nguvu amenitendea makuu. Na Jina Lake ni takatifu. Na rehema Zake hudumu vizazi hata vizazi. Kwa hao wanaomcha. Amefanya nguvu kwa mkono Wake; Ametawanya walio na kiburi katika mawazo ya mioyo yao. Amewaangusha wakuu katika viti vyao vya enzi. Na wanyonge amewakweza. Wenye njaa amewashibisha mema. Na wenye mali amewaondoa mikono mitupu. Amemsaidia Israeli mtumishi Wake; Ili kukumbuka rehema Zake. Kama alivyowaambia baba zetu, Ibrahimu na uzao wake hata milele." Mariamu binti mdogo hakuelewa mengi, ila alikuwa mnyenyekevu, na akajitahidi kuwa mcheshi, japo alikuwa na mawazo na shida zinazomzunguka. Ucheshi wa mama ni muhimu kwa mtoto.

*Lazima tutenge muda wa Kuomba — Tunapaswa sasa kujifunza na kujizoeza kumfahamu MUNGU kwa kuthibitisha ahadi Zake. Malaika wanatunza kumbukumbu ya kila sala ambayo ni ya dhati na ya kweli (Malaika wanarekodi kila ombi). Ni bora kutupilia mbali matakwa yetu ya binafsi kuliko kupuuzia ushirika na MUNGU. Umasikini wa kilindi kirefu, kujikana nafsi kwa kwa hali ya juu, vikiwa na kibali Chake, ni bora kuliko utajiri, heshima, maisha rahisi, na marafiki bila kibali Chake. Ni Lazima tuchukue muda na kuutenga kwa kwaajili ya kuomba

---

Maswali: Malaika alimwambiaje Mariamu? Mariamu alijibuje? Mariamu alimsifuje BWANA alipokuwa kwa Elizabeti? Somo hili linatufundisha nini? Wewe unafikiri Kwa nini Mariamu alichaguliwa kuwa mama wa Yesu?

**SIKU YA 193.**
**(Julai 11)**

# Kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji msafisha njia wa Masihi.

**Luka 1.**



Zamani za Herode mfalme wa Uyahudi kulikuwa na kuhani aitwaye Zakaria na mke wake Elizabeti alikuwa wa uzao wa Haruni. Walikuwa watu wa haki mbele ya Mungu , wakifuata maagizo na amri za Mungu bila lawama. Walikuwa hawana mtoto, maana Elizabeti alikuwa tasa na wote wawili walikuwa wazee sana. Akiwa katika zamu yake ya ukuhani, mbele ya Mungu, kura ilimwangukia kufukiza uvumba patakatifu, na mkutano wote ulikuwa nje ukisali. Zakaria alitokewa na malaika wa BWANA na akafadhaika, hofu ikamwingia; lakini yule malaika akamwambia “usiogope Zakaria maana dua yako imesikiwa, na mkeo Elizabeti atakuzalia mtoto mwanamume na jina lake utamwita Yohana. Nawe utakuwa na furaha na shangwe”, na watu wengine watafurahi kuzaliwa kwake, maana atakuwa mkuu kwa BWANA.

Mtoto huyu hatakunywa divai, wala kileo, naye atajazwa Roho Mtakatifu toka tumboni mwa mamaye, naye atawarejeza wengi katika Israeli kwa BWANA Mungu wao. Mtoto huyu atatangulia katika roho ya Eliya na nguvu zake, ili kugeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwasaidia waasi akili za wenye haki, na kumwekea BWANA tayari watu waliotengenezwa; ili Masihi akifika wawe tayari kumpokea.” Zakaria akauliza atajuaje kama haya mambo ni kweli, maana alikuwa mzee na mke wake ni mkongwe wa siku nyingi. Malaika akamtajia jina lake kuwa ni Gabrieli “Nisimamaye mbele za Mungu maana nimetumwa niseme nawe, na kukupasha habari hizi njema. Na tazama! Utakuwa bubu, usiweze kusema mpaka siku ile yatakapotukia hayo, kwa sababu huyasadiki maneno yangu; nayo yatatimizwa kwa wakati wake.

Huku watu waliobakia walikuwa wakishangaa, maana walimngoja kuhani wao aliyeenda kufukiza uvumba, wasimwone! Mwishowe kuhani alitoka wala hawezi kusema nao, hapo walitambua ya kuwa ameona maono ndani ya hekalu, naye aliwaashiria kama bubu, asiweze kusema. Alipomaliza huduma aliendo nyumbani kwake, na mke wake akachukua mimba akatawa miezi mitano akisema, Mungu

amemtendea mema kwani amemwondolea aibu yake ya kuitwa tasa mbele ya watu, maana siku zile watu walimsema au kumsuta mtu asiyekuwa na mtoto akajiona duni au mkosaji.

Mariamu aliharakisha kwenda, milima ya Yuda kumwona Elizabeti binamu yake. Njiani pengine alijiuliza kama yale malaika alimwambia ni ya kweli. Elizabeti alikuwa rafiki aliyemtuliza kwenye shida na aliyempenda Mungu na hivyo waliweza kutiana moyo katika habari hizi nzito na njema. Hata leo nawe ukipata habari za ajabu na nzuri kama hivi unaenda kumwambia nani? Tafuta yule atakayekutia moyo kwa yale bora. Basi alipofika kitoto kilicho tumboni mwa Elizabeti kikaruka. Mariamu alikaa miezi mitatu na kurudi kwake Nazareti, kwani hawakukaa karibu sana. Ikawa siku ya kuzaa Elizabeti zilitimia. Elizabeti alifurahi kuwa na binamu Mariamu wakizungumza, furaha zao, maana hakuweza kuzungumza na mume aliyekuwa bubu. Ilikuwa ni kuandika na kuashirikiana mambo kila siku. Kila mtu anapenda kuzungumza zaidi ya kuandika, maana huitaji karatasi wala kalamu au vifaa bali mdomo tu.

Elizabeti akajifungua mtoto mwanamume jirani waliposikia wakamsifu BWANA kwamba amemwongeza rehema Zake, wakafurahi pamoja naye, maana alikuwa mzee na tasa. Ikawa siku ya nane wakaja kumtahiri mtoto, wakataka kumpa jina la babaye Zakaria. Mamaye akasema, "La! sivyo, bali, ataitwa Yohana." Wakamwambia, Hapana mtu katika jamaa zako, aitwaye jina hilo. Wakamwashiria babaye wajue watakavyomwita, naye akataka apewe kibao aandike kwani alikuwa bubu. Alipopewa kibao aliandika "Yohana." Wakastaajabu jamaa wote, na mdomo wake ukafunguka papo hapo, akaanza kunena na kumsifu Mungu.

Watu wakaingia hofu, wote waliokuwa wakikaa karibu nao, na maneno haya yakasambaa katika nchi yote ya milima ya Uyahudi. Wale waliosikia waliyaweka maneno haya mioyoni mwao, wakisema "mtoto huyu atakuwa wa namna gani?" Kwa sababu mkono wa BWANA ulikuwa pamoja naye. Zakaria babaye akajazwa na Roho Mtakatifu na kutabiri akisema "Atukuzwe Mungu wa Israeli kwa vile amewajia watu wake na kuwakomboa, na kusimamisha Pembe ya wokovu katika mlango wa Daudi mtumishi wake. Yale alisema kupitia manabii watakatifu kuwaokoa kutokana na adui zao na kulikumbuka Agano Lake takatifu alilomwapia Ibrahimu.

Akasema mtoto wake huyu Yohana ataitwa nabii wa Aliye juu maana atatatangulia mbele ya BWANA au Masihi na kutengeneza njia Zake, awajulishe watu wake wokovu katika kusamehewa dhambi zao kwa njia ya rehema za Mungu. Akasema mwangaza umefikia wakaao katika giza na uvuli wa mauti na kuiongoza miguu yao kwenye njia ya amani. Yohana Mbatizaji akakua na kuongezeka Nguvu rohoni, wakampeleka akae nyikani, na si mjini, hata siku ya kutokea kwake Israeli.

Tunaposoma kuzaliwa kwa Yohana tukumbuke kwamba Mungu ana mpango na kila mtoto au mtu mzima, kama baba yetu. Jambo kubwa la maisha yetu liwe kujua kwamba Mungu ana mipango gani kwetu ili tuishi na kutimiza mipango hiyo maalumu.

*Tumia muda mwingi katika Maombi — Tumia muda mwingi katika maombi na kutafuta kwa ukaribu Neno. Hebu wote wapate Ukweli halisi wa imani katika mioyo yao kwa kuamini kwamba Roho Mtakatifu atamwagwa kwao kwa sababu wana njaa halisi na kiu ya haki. Wacha kuwe na maombi zaidi, kuamini, na kupokea, na kufanya kazi zaidi pamoja na MUNGU.


---------------------------------------------------

Maswali: Malaika alimwambia nini Zakaria? Zakaria alitoa udhuru gani? Elizabeti alipomwona Mariamu nini kilitokea? Watu walijuaje jina la mtoto litakuwa Yohana? Nabii wa aliye juu ina maana gani? Jina Yesu au Yeshua, lina maana gani?

**SIKU YA 194.**
**(Julai 12)**

# Kuzaliwa kwa Yesu Masihi na Mwana wa Mungu.

**Luka 2 na Mathayo 2.**



Siku zile amri ilitoka kwa Kaisaria Agusto wa Rumi, aliyetawala dunia yote ya wakati huo, ikatangazwa kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote ulimwenguni yaani sensa ili kila mtawala ajue ana raia wangapi wako chini yake. Orodha hii ndiyo ya kwanza iliyoandikwa wakati huo. Sensa ilifanywa ili kukusanya kodi, au kujua watu au raia wa umri wa kuweza kwenda vitani. Watu wote wakaenda kuandikwa kutokana na mji wao au ukoo wanapotoka. Yusufu wa ukoo wa mfalme Daudi, akaondoka toka Galilaya mji wa Nazareti ili aende Bethlehemu ya Uyahudi, kilomita zaidi 120, kwenye mji alikozaliwa mfalme Daudi, maana alikuwa wa ukoo ya Daudi.

Walienda waandikwe na Mariamu aliyekuwa amemposa naye alikuwa na mimba. Yusufu alifunga ndoa na Mariamu, alipopata ndoto toka kwa Mungu. Safari hii ya kupanda punda, kwenye mabonde na miinuko kwa mama anayetegemea kujifungua haikuwa rahisi. Cha kujifunza hapa, ni kwamba wazazi wa Yesu walikuwa watu ambao waliishi kwa amani wakitunza sheria za nchi zisizopingana na imani yao. Mariamu alikuwa ameposwa na Yusufu kabla hawajakaa kama mke na mume alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Yusufu aliyekuwa amemposa, alikuwa mtu wa haki, na asitake kumwaibisha, na pia alimpenda Mariamu, aliazimu kumwacha kwa siri.

Pengine Mariamu alipomwambia hakuamini kwani jambo kama hili halijawai kutokea, na haliwezekani. Ndiyo maana malaika alimwambia Mariamu alipouliza

nitapataje mtoto na sina mume? Malaika alisema "Kwa Mungu vyote vyawezekana." Yusufu alijua Mariamu ni msichana mwaminifu, "sasa nini kimetokea" au "ni mwanamume gani amempenda kuliko mimi?" Mariamu alikuwa msichana wa miaka 14 mpaka 17 hivi. Yusufu angeweza kumpeleka mahakamani siku zile, maana kuposwa, ilikuwa kama ndoa kwa sheria yao, na angeweza kisheria auwawe, kutokana na sheria ya Musa. Ila hakupenda kumfanyia lolote baya Mariamu, na wakati huo huo hakupenda kumchukua msichana ambaye amezini na mtu mwingine. Akafikiri pengine angempa talaka, au apotee na kumwacha kimya kimya. Hapa tunapata hekima wakati watu wametutendea mabaya, hakuna haja ya kuwaaibisha au kupayuka!

Alipokuwa akifikiri hivi, tazama, malaika wa BWANA akamtokea katika ndoto, akisema "Yusufu mwana wa Daudi usihofu kumchukua Mariamu, kuwa mkeo, maana mimba yake ni kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Naye atazaa Mwana, nawe utamwita Jina Lake Yesu, maana Yeye Ndiye Atakayewaokoa watu Wake na dhambi zao. Hayo yote yamekuwa, ili litimie Neno lililonenwa na BWANA kwa ujumbe wa nabii akisema 'Tazama bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita Jina Lake Imanueli; Yaani Mungu pamoja nasi." Naye Yusufu alipoamka katika usingizi alifanya kama malaika wa BWANA alivyomwagiza, akafunga ndoa na akawa mkewe, asilale naye kitanda kimoja mpaka alipomzaa mtoto.

Imepita miaka 2,000 toka Mariamu alipoambiwa habari hizi, ila Maneno haya yana maana kuu hata leo pia. Yesu alizaliwa kutuokoa dhambini binadamu wote, wafupi au warefu, matajiri au masikini, waafrika au wazungu na Wahindi. Basi hapo ndipo Yusufu alifanya harusi na kumchukua Mariamu. Lazima wazazi hawa, nao mara zingine walifikiri Yesu atakuwa mfalme na kuwasaidia kutoka utumwa wa Warumi au umasikini! Walichukua jukumu zito, 'kumbeba Mungu', kumlea katika mambo yote unayoyajua mzazi anamfanyia mtoto. Mfano kumlisha, kumlaza, kuwongesha, kumvalisha na kadhalika. Akili finyu zinapofikiri haya, tunabakia midomo wazi tu kwa huu upendo wa Mungu. Mfano mdogo wa kujaribu kuelewa, ni kama leo wewe uwapende sana siafu, mpaka uamue kuzaliwa kama siafu, na kuishi kama siafu, ufe kwa ajili ya siafu, na kisha ubaki na umbo la siafu milele zote.

Yusufu na Mariamu walipojua wote wamechaguliwa na kutunukiwa na Mungu kitu cha thamani kuliko vyote duniani na mbinguni; yaani Mwana Wake, na kwamba mbingu yote imemiminwa nyumbani mwao, walifurahi kwamba japo jukumu hili ni gumu, na hawakulielewa vyema, hawakujali ugumu wala masengenyo ya watu tena. Hata leo nawe Je wajali watu wanakusengenya "eti anajidai anampenda Mungu na kushika maagizo Yake!." Yusufu hazungumzwi sana ila kama Baba alikuwa na jukumu kubwa la kumchukua Mariamu kila mahali, kumlinda, kumsaidia Mariamu, kumlea Yesu, kumfunza ustadi ili awe na kibarua na mengineyo mengi ambayo baba zetu wanatufanyia, kwani inachukua wazazi wawili kumsaidia mtoto.

Ikawa katika safari hiyo ya Bethlehemu, na siku za kuzaa zikatimia. Watu walikuwa wengi kufuatia agizo la sensa, na hoteli zote zilikuwa zimejaa. Kwa vile Yusufu na Mariamu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni, mtu aliyewahurumia aliwapa zizi lake la wanyama. Wakunga wa jadi, au wakina mama rafiki zao wa Nazarethi

hawakuwepo hapa. Mariamu akamzaa Mwana, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori au chombo cha kulia ngombe, pengine lichuma au boksi la mbao chafu chafu hivi. Mwana-Kondoo wa Mungu (Mtoto wa kondoo) alikuwa katika nyumba ya kondoo. Kuzaliwa kwa Yesu kati ya wanyama, kumenipa picha kumbe Mungu anawathamini wanyama kuliko tunavyofikiri!

Wanyama walikuwa tayari kumkaribisha, makaoni mwao, bali binadamu walikuwa hawana nafasi. Watoto wengi siku hizi huzaliwa hospitali ila Yesu alizaliwa kwenye zizi. Pengine wazazi Wake wa duniani walishangaa Kwa nini iwe hivi, na kwa nini wao masikini wachaguliwe kumtunza mtoto yule, mwenye utajiri wote? Hata watu masikini leo huzaliwa ndani ya nyumba, maana wengi wana huruma kwa mama anayejifungua, hawawezi kumweka kwenye zizi. Maambukizo kama ya tetanus kwa kitovu cha mtoto mdogo na mama ni mambo mengine ya kutisha! Ila Mungu alipenda na akatoa kila kitu, na kisha anaendelea kutoa hadi leo.

Tumefikiri, hata Yusufu seremala, je asingeweza kutengeneza kitanda cha mtoto na kutayarisha kama wazazi wengine? Yesu alishuka chini kabisa, kama tunavyoona kwenye Wafilipi mbili. Basi wale wote ambao ni masikini mno wa vitu vya duniani, tujipatie faraja na jambo hili. Tunapofikiri vyote Yesu alivyoacha kwa ajili yetu au kwa ajili yangu, tumejiuliza sisi au mimi nitaacha nini kwa ajili Yake? Jiulize leo, je una nafasi katika moyo wako kwa Yesu? Ili tusije kuwa kama Bethlehemu iliyokosa nafasi usiku ule kwa Mfalme wa wafalme alipozaliwa. Lazima tuwe makini na kisa hiki, na kukata ushauri kuishi tofauti. Tunaposherekea Krismasi, tukumbuke inahusu nini. Isiwe ni sherehe ya ulafi, na ulevi tu, bali tuitumie kuwapa pesa na muda wetu wenye mahitaji na kupitia kukisoma kisa hiki tena na tena! Na si kubadilishana zawadi ambazo hatuzihitaji, au kukata miti ambayo haitukumbushi maana halisi ya kisa hiki!

Si kila mtu alikuwa amelala. Katika nchi hiyo kulikuwa na wachungaji masikini makondeni wakifanyiana zamu kuangalia makundi usiku. Ghafla malaika wa BWANA akawatokea, na utukufu wa BWANA ukawang'aria pande zote, ikawa kama mwanga wa mchana, wakaingiwa na hofu kuu. Malaika akasema "msiogope kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa Masihi, kwa ajili yenu, Mwokozi Ndiye Kristo BWANA. Hii ndiyo ishara kwenu; mtakuta Mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ngombe." Ghafla likatokea Jeshi kubwa la malaika wa mbinguni, wakimsifu Mungu na kuimba.

Yawezekana maelfu au mamilioni ya malaika waliimba siku ile. Kumbe nyimbo ni muhimu sana; Je watu wakiimba kanisani au nyumbani mwako, wewe wakaa kimya au unajiunga nao? Nyimbo za kumsifu Mungu ni muhimu. Weka muda wa kumsifu Mungu kwa nyimbo kila siku iwe ni tenzi, Zaburi, ama nyimbo za kawaida kama tunavyoshauriwa kwenye mafungu haya; Wakolosai 3:16 na Zaburi 104:33. Biblia imezungumza kuhusu kwaya za watu 4000 zilizokuwa zinamsifu Mungu. Uimbaji ni Uinjilisti, usiwe mwimbaji wa kwaya bila kusoma Neno la Mungu. Lazima uimbe kwa akili au ufahamu! Nyimbo zako zivuviwe! Chagua kwa makini nyimbo zako, usijiingize kuimba nyimbo zisizomtukuza Mungu, au zinazomsikitisha. Mungu

anapendezwa na kuishi katika sifa za watu Wake. Yesu alipozaliwa Mungu hakutoa mahubiri bali aliwaambia malaika waimbe kutuonyesha umuhimu wa nyimbo. Watoto wengi hupenda kuimba, hebu shauku hii iendelee mpaka uzeeni. Hata Mungu BABA huimba pia.

Malaika wakaimba "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia." Ikawa malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji wakaambiana "Twendeni mpaka Bethlehemu, tukalione hilo lililofanyika, alilotujulisha BWANA." Wakaenda haraka, na kumkuta Mariamu, Yusufu na yule mtoto mchanga amelala horini. Wakawasimulia vile walivyoelezwa na malaika. Malaika hawakuwatokea maofisa fulani, bali watu wadogo, watumishi, au watumwa, wanaochunga mifugo ya watu. Watu hawa wengi wao hawakujua kusoma, na pengine hawakuwa nadhifu sana kwaajili ya kazi za mifugo, ila walikuwa wanyeyekevu na Mungu alitaka kuwaonyesha anajua shida zao. Inaonekana wengi walikuwa wameajiriwa, yaani hawakumiliki ile mifugo!

Wachungaji walikuwa si wanyenyekevu tu, bali watu ambao wako tayari kuwaambia wengine matendo makuu ya BWANA, ili wengi wapate uzima wa milele. Yesu ni wa watu wote, si wa kanisa fulani, au watu fulani, ni wetu binadamu wote, alikuja atuokoe kutoka kwenye dhambi zetu, hebu tushangilie binadamu wote! Wachungaji kumwona Yesu horini, kulibadilisha maisha yao milele, na sisi pia leo, tunavyokutana na Yesu, fumbo la upendo wa Mungu kwetu linafumbuka. Basi tuwe waangalifu, maana dini mara nyingi ni mpango wa mwanadamu kumfikia Mungu, ila Ukristo ni mpango wa Kristo Kumfikia mwanadamu na upendo Wake!

*Omba, ndiyo, omba kuliko ulivyowahi kuomba maishani mwako, ili usidanganywe na hila za Shetani, ili usipate kuangukia ugonjwa wa moyo usiokuwa na usikivu, moyo usiojali, na wenye ubatili, na kisha ujihudhurishe kwenye majukumu na shuguli za kidini kwaajili tu ya kutuliza dhamiri yako mwenyewe.

---

Maswali: Kwa nini Yusufu na Mariamu walienda Bethlehemu? Malaika aliwaambiaje wachungaji? Je malaika kama wale wa Bethlehemu wapo nasi siku hizi? Jeshi la malaika liliimba wimbo gani? Je ni nyimbo au muziki wa aina gani unamsikitisha Mungu? Kwa nini Mungu aliwatokea watu masikini, waliochunga mifugo ya watu na si matajiri kwenye majumba ya kifalme? Hori ina maana gani? Je ungejisikiaje kama wazazi wako wangechaguliwa kumzaa Yesu, na mdogo wako awe Yesu? Je mwenye hoteli angejua kwamba Yesu ni Masihi angefanya lipi kumsaidia kuepuka mazingira hori?

**SIKU YA 195**
**(Julai 13)**

# Mamajusi kutoka mashariki wamtembelea Yesu

**Mathayo 2.**



Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi ilikuwa wakati mfalme Herodi anatawala, na tazama mamajusi, yaani watu wenye hekima, cheo, waungwana na wenye elimu ya nyota, sayansi na utabibu; walikuja kumwona kutoka nchi za mashariki, wakiangalia nyota na wakafika Yerusalemu wakiuliza "Yuko wapi Yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliona nyota Yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia." Hawa walikuwa wamesoma unabii wa Baalamu wa kitabu cha Hesabu, na manabii wengine, na kujua mambo ya nyota.

Roho wa Mungu aliwaita toka kwao wakapanda ngamia au farasi kusafiri usiku tu ili wapate kumwona Yesu. Walipoona nyota hiyo waliifuata mpaka Yerusalemu. Walifikiri kama wao watu wa nchi za mbali wamejua kuzaliwa kwa Mwokozi, basi WaIsraeli watakuwa na habari za kutosha, kumbe masikini wengi miongoni mwa WaIsraeli walikuwa wamerudi nyuma kwa mambo ya kiroho, hivyo hawakujua kinachoendelea. Mungu aweza kumpita mtu anayeonekana amekolea dini aende kwa mtu mnyenyekevu aliye tayari kusikia asiyeonekana kama ana dini. Hata hivyo Mungu aliwapa nafasi wale walioulizwa kufikiri na kutafuta jambo hilo kama ni la kweli.

Mamajusi waliona habari za kuzaliwa kwa Mwokozi ni za furaha mno, wakashangaa namna zilivyowatia Wayahudi hofu. Mfalme wao Herodi aliyetawala japo alikuwa mkongwe aliposikia, alifadhaika na uongozi wake, kwamba kuna Mfalme zaidi ya yeye na atamtoa kwenye kiti, japokuwa alikuwa mkongwe alikuwa na tamaa ya mamlaka. Hata kabla Yesu hajaanza kutembea alikuwa anatafutwa tayari kama mtuhumiwa. Hili lafanya tujue maisha ya Yesu yalikuwa magumu sana kuzidi yetu. Herodi akakusanya makuhani wote na waandishi, akatafuta habari kwao kama haya ni ya Kweli, akauliza "Kristo amezaliwa wapi?" Nao wakamwambia kutokana na Maandiko, ni Bethlehemu ya Uyahudi. Nabii Mika aliandika "Nawe Bethlehemu ya Yuda, hu mdogo kamwe Kwa kuwa kwako atatoka Mtawala atakayewachunga watu Wangu Israeli." Unabii wa Daniel nane na tisa ulieleza wazi mwaka atakapozaliwa, atakapobatizwa au kusimikwa na atakapokufa.

Wayahudi walikuwa wamemfukuza Roho wa Mungu asiwashauri wakawa vipofu kwa tukio hili kuu. Japo Bethlehemu ilikuwa km 12 tu toka Yerusalemu hawakwenda, wala kuchunguza na kuuliza yale mamajusi waliyosema, bali waliendelea kuonyesha wazi hawajali kabisa. Hawakuwa wajinga kwa ujuzi wa Maandiko, na hivyo walijua utabiri wa Masihi. Wangefanya utafiti kidogo tu, kwa nia njema, Mungu angewaonyesha wazi. Ni Roho Mtakatifu alikuwa hayumo katika maisha yao. Hata leo tuwe Makini, maana makanisa mengi, Roho wa Mungu akiondolewa hakuna atakayeng'amua, shuguli za makanisa zitaendelea kama kawaida, iwe ni mahubiri, huduma za jamii, au nyimbo.

Maelfu ya malaika waliimba Bethlehemu, lazima kuna wengi waliosikia usiku ule nyimbo zile tamu. Hatudhani kwamba malaika kuimba angani ilikuwa siri, lazima walikuwa wanawaimbia watu, na si mbingu tu. Wayahudi waliposoma Maandiko, kujifunza kwao kukawa uangamivu kwani walitaka waonekane wana haki, bali nia na mawazo yao yalikuwa yana uovu.

Basi Herodi akawaita mamajusi kwa faragha awaulize "Je waliona nyota ile lini?" maana walisafiri muda wa miezi baada ya kuona nyota, na kufunuliwa na Mungu kwamba Masihi anazaliwa. Mamajusi wakamwambia, na akapata muda ule, ndipo Herodi akawapeleka Bethlehemu akasema washike njia na kuuliza sana mambo ya mtoto na wakiisha kumwona waje kumletea habari ili naye aende kumsujudia. Huu ulikuwa ni udanganyifu, kwani alitaka kumwua Mtoto Yesu, akifikiri atampindua.
Masikini hakujua huyu ni Mfalme wa wafalme aliyejishusha na kuzaliwa kama mtu ili amwokoe yeye na sisi sote kutoka katika dhambi zetu milele zote. Huyu hakuwa mfalme wa siasa au serikali za kibinadamu. Yeye alikuwa anafikiri ufalme wake mdogo badala ya mabilioni ya sayari. Herodi huyu alijulikana kwa ukatili, hata kuua watoto wake, japo alikuwa ni wakabila la Edomu (Idumea) mke wake alikuwa ni Myahudi wa damu ya kifalme. Herodi huyu aliua watoto wake kwa wivu. Yasemekana Kaisari Agusto alitamka siku moja 'kuna unafuu kuwa nguruwe wa Herodi utapona kuliko kuwa mwana wa Herodi' maana alikuwa na wivu na ukatili. Mamajusi waliposikia maneno ya mfalme walishika njia na tazama ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia hata ikaenda kusimama pale alipokuwa mtoto. Mamajusi walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kuu mno, wakaingia nyumbani na kumwona mtoto, pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia.

Mfalme wa wafalme alikuwa hana mlinzi, askari au mpambe. Mariamu na Yusufu wakashangaa. Wakafungua hazina zao na kumpa tunu za dhahabu, uvumba na manemane. Vitu hivi vilikuwa vya thamani siku zile, hesabu ya mamajusi haisemwi, pengine walikuwa wengi, ila zawadi zilikuwa za aina tatu yaani uvumba, manemane na dhahabu. Kwa maneno mengine, maandiko haisemi walikuwa watatu, ila zawadi zilikuwa tatu!

Mamajusi Walikuwa wamesafiri kwa muda, na bado walikuwa wana zawadi. Hawa walikuwa wakimcha Mungu, na walimwomba Mungu waweze kumwona Masihi kwa kuwa inaelekea walikuwa wamesoma unabii wake uliotabiriwa katika kitabu cha Danieli 9. Nao wakiisha kuonywa na Roho wa Mungu katika ndoto, hawakumrudia Herodi, bali wakaenda zao kwa njia nyingine. Hata leo watu wenye hekima bado wanamtafuta Yesu na kumpa zawadi. Mtoto huyu Ndiye Yule Masihi aliyeahidiwa; kwa Musa alimwambia, MIMI NDIYE, Daudi alimwita Nyota ya Asubuhi, manabii wengine walimwita Tumaini ya vizazi vyote. Yesu ni tumaini la binadamu wote haijalishi madhehebu. Maana wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Twahitaji Mwokozi.

Mara nyingi tunazungumzia Historia ya Yesu na kusahau kuzungumzia kuhusu wito Wake wa kushuka chini na kusaidia maskini, wenye shida na wenye maumivu. Yesu alikuwa tayari kusaidia maskini na wenye maumivu, nasi leo tuna jukumu la kufanya vivyo hivyo. Mada ya upendo ndiyo imetawala milki ya Mungu. Siri na fumbo la Upendo wa Mungu, kutuokoa sisi wanadamu, litazungumzwa na malaika milele zote, nasi binadamu tutaimba milele zote tukiendelea kujifunza maisha Yake na wokovu aliotupa. Katika Yesu tunaona kwamba furaha kubwa ya Mungu na utukufu Wake ni kutoa.

Mamajusi walipoenda, Malaika wa BWANA akamtokea Yusufu katika ndoto, akamwambia aondoke, amchukue mtoto na ukimbie Misri, ukae kule mpaka Mungu aelekeze kurudi, maana Herodi alikuwa anamtafuta mtoto amwangamize. Yusufu, Mariamu na mtoto Yesu wakaenda Misri, katika bara la Afrika ili litimie neno la nabii Hosea "kutoka Misri nalimwita mwanangu." Zamani zile ilikuwa mbali kwenda na punda km 300 hivi ili wafike Misri. Yesu alianza kuchukiwa na kutafutwa auwawe toka kuzaliwa kwake. Shetani alitaka kumwangamiza ili tusipate wokovu.

Zile zawadi za kifalme walizotoa mamajusi, zikawa msaada kwao nchi ya ugeni Misri kuwawezesha kuishi. Maandiko hayasemi ila wanahistoria wasema walikaa Misri miaka mitatu hivi. Herode mkuu alipoona amedhihakiwa na wale mamajusi akaghadhabika na kuwatuma watu kuwaua watoto wa kiume wa pungufu ya miaka miwili; waliokuwa Bethlehemu na viungani mwake, ndipo lilipotimia Neno la nabii Yeremia "Sauti ilisikiwa Rama, Kilio na maombolezo mengi, Raheli akiwalilia watoto wake, Asikubali kufarajiwa kwa kuwa hawako." Wazazi walikuwa na huzuni nzito. Wivu unafanya ubongo usifanye kazi. Mtu mkongwe kuua watoto wadogo kwa hofu kwamba watampindua kwenye ufalme, bila kufikiri kwamba wakikua atakuwa ameshaaga dunia. Herodi alikufa miaka michache baadaye, au tuseme muda mfupi baada ya kuua wale watoto wa Bethlehemu.

Malaika wa BWANA alimtokea Yusufu na kumwambia arudi na mtoto na mama Yake “maana waliomtafuta kumwua wamekufa.” Yesu alibebwa alipokuwa anaenda uhamishoni Misri, lakini sasa alikuwa anarudi ameshakuwa mkubwa wa kutembea Mwenyewe. Wakafurahi wanarudi kwao kuwaona watu wa kwao. Basi akaondoka na kurudi Israeli, na aliposikia Mfalme Arkelao, mtoto wa Herode anamiliki Uyahudi aliogopa kwenda huko. Lakini baada ya kuonywa katika ndoto, akasafiri Galilaya, na akaenda kukaa katika mji unaoitwa Nazareti, ili litimie Neno la unabii “ataitwa Mnazarayo.” Shetani alionyesha chuki na hasira kubwa mbinguni kwa kuleta uasi, akitaka amtoe Mwenyezi Mungu kwenye kiti Chake na kumwua Yesu, ila tunashukuru Mungu aliyeshinda yote.

Kisa cha mamajusi ni fundisho kwetu jinsi tunavyomtendea Yesu. Kuna jinsi tatu tu za kutenda; kumkataa, kumwabudu, kumkaribisha mioyoni mwetu au kutoonyesha kujali. Kuwa mshiriki wa kanisa ni vyema, ila haimaanishi kwamba mahusiano ya mtu huyo yako sawa na Mungu. Mungu anatupa nafasi na uhuru wa jinsi tunavyotaka kumtendea “Mfalme wa Wayahudi” ambaye leo tunamjua kama “Mfalme wa Wafalme” Yesu Masihi.

*Ombeni Daima - “Ombeni kila wakati;” hiyo ni kwamba, Daima uwe katika roho ya maombi, na hapo ndipo utakapokuwa tayari kwa Ujio wa Bwana wako.
-------------------------------------------------------

Maswali: Ni nani walimtembelea mtoto Yesu wakiwa na zawadi? Kwa nini Herodi aliogopa kuzaliwa kwa Yesu? Herodi alitafuta habari wapi za kuzaliwa kwa Masihi? Herodi aliwaambiaje Mamajusi? Kwa nini ni vigumu kuacha ufalme na kuzaliwa kwenye nyumba ya ng’ombe? Zawadi za Mamajusi zilitumikaje? Kama malaika waliimba wakati wakitoa habari njema, Je, huwa ni sawa kukaa bila kuimba tunapoagizwa kuimba kanisani?

**SIKU YA 196**
**(Julai 14)**

# Yesu abarikiwa hekaluni akiwa na siku 40.

**Luka 2.**



Wazazi walimchukua Yesu hekaluni, akiwa na umri wa siku nane. Kubarikiwa Kwake kulifanyika kabla ya Mamajusi kumtembelea mtoto, maana wazazi wasingerudi Yerusalemu kujionyesha kwa Herodi ili wawe shidani kuuwawa. Wachungaji walioenda kumwona mtoto Yesu, walitoa habari waliyoambiwa juu ya huyo mtoto. Wote waliosikia wakastaajabu kwa hayo waliyoambiwa na wachungaji. Lakini Mariamu akayaweka Maneno haya yote, akiyafikiri moyoni mwake. Wale wachungaji wakarudi, huku wakimtukuza Mungu na kumsifu kwa mambo yote waliyosikia na kuyaona, kama walivyoambiwa.

Hata zilipotimia siku nane wazazi walimtahiri Naye akaitwa Jina lake Yesu kama alivyoitwa na malaika kabla hajachukuliwa mimba. Hata zilipotimia siku za kutakasika kwao, kutokana na Torati ya Musa, yaani siku 40 kwa mvulana, walikwenda Yerusalemu ili wamweke wakfu kwa BWANA; kama ilivyo sheria ya BWANA, "mtoto wa kwanza mwanamume anaitwa mtakatifu kwa BWANA." Wakatoa sadaka ya njiwa wawili kwa vile walikuwa masikini. Wale wenye uwezo,

walitoa sadaka ya kondoo. Kuhani alifanya wajibu wake, bila kujua Mtoto huyu ni nani, pengine aliona hawezi kuwa Masihi, maana wazazi Wake ni watu wa kipato cha kawaida tu.

Watu walikuwa wanatarajia Masihi awe tajiri na mwenye nguvu, za kuondoa maudhi yao yote. Utaratibu wa kutoa sadaka ya shukrani kwa ajili ya mtoto au katika siku ya kuzaliwa, unafaa kutumiwa hata leo. Mitindo ya kileo tuliyoigiza toka magharibi ya kusherekea siku ya kuzaliwa, kwa kutumia pesa kwa fujo au kubugia vitu peke yake ni kitu ambacho hakina mvuto mzuri kwa wanaomcha Mungu.

Na tazama pale Yerusalemu kulikuwa na mtu mmoja akiitwa Simeoni, mtu mwenye haki na mcha Mungu, akitarajia faraja ya Israeli, na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake. Huyu alikuwa amefunuliwa na Roho Mtakatifu ya kwamba hatakufa mpaka amwone Kristo Masihi wa BWANA kwa macho yake mwenyewe. Basi Simeoni akaja, hekaluni akiwa ameongozwa na BWANA, na wale wazazi wa Yesu walipomleta mtoto awekwe wakfu, wakamwona Simeoni anakuja upande wao na kuwapokea Mtoto mikononi mwake. Wazazi wakashangaa na wakampa Mtoto, kisha akanena “sasa BWANA wamruhusu mtumishi wako, alale kwa amani, kama ulivyosema; kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako, Ulioweka tayari machoni pa watu wote; Nuru ya kuwa mwangaza wa mataifa, na kuwa utukufu wa watu Wako Israeli.”

Yusufu na Mariamu wakastaajabia hayo yaliyonenwa na mzee huyu. Kisha Simeoni akawabariki wale wazazi na kumwambia Mariamu mama Yake Yesu “Tazama huyu mtoto amewekwa kwa kuanguka na kuinuka wengi walio katika Israeli, na kuwa ishara itakayonenwa. Nawe upanga utaingia moyoni mwako ili yafunuliwe mawazo ya mioyo mingi.” Huu unabii wa Simeoni ulikuwa una maana kwamba Masihi atakubaliwa na wengi, ila wengine watamkataa. Kule kumkataa, kutaonyesha hali yao ya kiroho iko chini na hivyo wataanguka. Si kwamba Mungu atawahukumu watu, ila watu watajihukumu wao wenyewe kwa jinsi watakavyomtendea Yesu, huku wakianguka au kuinuka.

Unabii huu ulitimia kwani mafarisayo, makuhani na wengine walianguka, ila wengi waliinuka na kumkubali Yesu kama Masihi. Mamaye aliposikia ‘upanga utamchoma moyoni’ hakuelewa vizuri. Ila alipokumbuka maneno ya Simoni alipata faraja na kuendelea mbele. Utimilifu wa Maneno haya Mariamu aliuona katika maisha ya Yesu. Aliposikia watu wakimsema kwa mambo mbali mbali, alijiuliza, na hata shaka ikamwingia; na hasa alipomwona msalabani. Mariamu alitayarishwa na ujumbe wa Simoni kuhusu hili, maana wengi siku zile hakuwakuelewa vizuri kwamba Masihi atateswa na kuishi maisha ya huzuni kwa ajili yetu. Maisha ya Yesu hayakuwa na ubinafsi toka kuzaliwa mpaka kufa msalabani.

Mariamu alisikia mengi mabaya yaliyosemwa kumhusu Yesu. Mfano alisikia watu wakisema “mtoto wako anasali usiku kucha, na anafundisha watu wale hata bila kula”, na wengine walisema mwanao ana pepo. Marafarisayo japo walijua Torati na wangepaswa kuwa waangalifu kwa maneno yao, walimpa Mariamu huzuni nyingi. Hata leo twapaswa tuwe waangalifu kwa maneno yetu ya kashfa tunayozungumza kuhusu watu. Tusipojitoa kikamilifu kwa Mungu, tutakuwa na maneno ya kuchoma

au kuumiza wengine na mwishowe kukataliwa.

Maneno haya ya kutia uchungu hayakuwa yanatoka kwa mafarisayo na viongozi wa dini peke yao bali hata kutoka kwa ndugu zake, rafiki au watoto wa Mariamu. Yalikuwa na uchungu, na hata Yesu akasema adui wa mtu ni watu wa nyumbani mwake. Mariamu alichomwa hasa wakati Yesu alikataliwa na watu wa karibu. Pengine aliona ni bora akubaliane na Mafarisayo na wakuu wa dini ili kupunguza utesi kwao na kwake mwenyewe.

Familia iliyokuwa imlinde ikawa pia mwiba. Yesu ili kumpunguzia mamaye uchungu mara zingine alipenda kutembelea nyumba za wale ambao hawakuwa jamaa zake kama Lazaro, na dada zake. Pale alipata muda wa kusali bila kumpa mamaye uchungu. Hata leo watoto wengine wanapata shida ya kukataliwa, na kukasirikiwa, kwa sababu ya imani yao kwa Mungu. Hawa waweza kupata faraja kwa Yesu. Yesu ni jamaa yetu wa karibu kuliko baba, mama, dada, kaka au mpenzi yoyote. Hatuwezi kujua kwa kikamilifu upendo Wake, ila tunajua ni upendo halisi, na tunaweza kuwaonyesha wengine upendo huu.

Wengine hekaluni waliona ni siku ya kawaida kama nyingine tu; na hivyo wakaendelea na pilika pilika. Hata wale makuhani waliomweka wakfu mtoto, hawakujua lolote kwamba Mwana wa Mungu na Imanueli, yupo hapo hapo kati yao. Kusoma Maandiko, ni tofauti na kuishi Maandiko. Hata leo Mungu anapofunuliwa watoto Wake waliojiweka wakfu, huonyeshwa mambo makuu, hasa katika siku hizi za mwisho. Lakini mafunuo ya Maandiko tu, hayatoshi, tunapaswa tuyaishi hayo Maandiko!

Hapo hapo palikuwa na nabii mke aliyekuwa na miaka 84, jina lake Ana, binti Fanueli wa kabila la Asheri. Mumewe alikufa baada ya miaka saba, ya ndoa na aliishi miaka mingi ya ujane. Huyu hakuondoka hekaluni; bali alikaa usiku na mchana akiabudu, akifunga na kuomba. Ana alitokezea saa ile ile Simeoni akiwa pale na akamshukuru Mungu na wote waliokuwa wakiutarajia ukombozi katika Yerusalemu, akawatolea habari za Yesu. Walipomaliza yote yaliyotakiwa kufanya hekaluni ili kutimiza sheria ya BWANA, walirejea Galilaya mpaka mjini kwao Nazareti.

Wazee wawili masikini na wanyenyekevu walifungua mioyo yao kwa Masihi, ila viongozi wakuu wa Israeli walifunga macho yao, na hawakuona muujiza uliotokea mbele yao siku ile. Viongozi wengi siku hizi wanazungumzia kuhusu Yesu wa historia na kupuuzia wito Wake wa kusaidia masikini na wale wanaoteseka. Ni muhimu sana sote tunaomwamini, kuishi maisha ya kujinyima, na kusaidia wenye mahitaji, maana ndiyo kazi Yesu alikuja kuifanya. Alikuja kusaidia masikini wa kiroho na kimwili.
Naye mtoto Yesu akakua akiongezeka nguvu, akijaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu Yake akiwapendeza Mungu na wanadamu. Hii yaonyesha, Yesu Alikua kiakili, kimwili, kiroho, na kijamii. Huu ndiyo wakati alioenda Misri kukimbia vitisho vya Herodi na akawa mkimbizi huko. Na mji aliokuzwa wa Nazarethi nao ulikuwa haufai hata Nathanieli hakuweza kujizuia akasema “Laweza neno jema kutoka Nazareti?” Mara nyingi watu hulalamikia mahali walikozaliwa na hata watoto hulalamika kuwa tabia mbaya walizonazo zinatokana na kule walikokulia ambako

kumewafanya wawe na hasira, kutohudhuria ibada au kutompenda Mungu. Yesu hakutoa sababu kama hizi, alijua Baba wa mbinguni ana mpango na kila mtu, na akajua mpango Wake, na aliishi ili autimize mpango huo. Maisha Yake ya miaka 30 aliyoishi na wazazi Wake, ndiyo yaliyofanya huduma Yake iwe harufu ya manukato kwa Mungu.

Hata leo nawe, usidharau maisha yako nyumbani, kwani haya ndiyo matofali ya kujenga tabia. Je twaweza kujifunza hili nasi leo, ili tusione wivu, kwamba "bora tungezaliwa na tajiri fulani, au mtu fulani ndipo mambo yetu yangekuwa mazuri sana"
*Hitaji la Maombi mengi — Sasa kuna hitaji la maombi mengi. Kristo anaamuru, "Ombeni bila kukoma;" yaani, ielekeze akili yako juu kwa MUNGU, Chanzo cha nguvu zote na ufanisi.
----------------------------------------
Maswali: Kwa nini mchungaji aliyembariki Yesu hakujua huyu ni Masihi? Kwa nini Yesu alikimbizwa Misri? Simeoni alimwambia Mariamu Maneno gani? Nabii Hana ni nani? Mji wa Nazareti ulikuwa na sifa gani? Yesu alikua katika nyanja gani? Kwa nini Simoni alisema, Yesu ni Nuru ya mwangaza wa mataifa yote na si Israeli peke yake? Kwa nini Simoni alisema Yesu ni faraja ya Israeli? Jina la Yesu lina maana gani?

**SIKU YA 197**
**(Julai 15)**

# Yesu hekaluni akiwa na miaka 12.

**Luka 2.**



Biblia haisemi sana utoto wa Yesu au Isa bin Mariam, kwa sababu ambazo hatuzijui. Mungu amechagua kusema machache kwetu kuhusu utoto wa Yesu. Ila alirudi toka Misri akiwa na miaka pungufu ya tano. Akaishi nyumbani mpaka alipofika miaka 30. Pengine alizungumza Kiebrania, Kimisri, Kiyunani au Kirumi! Baba Yake alikuwa seremala, hivyo alisaidia kazi za nyumbani. Itakuwa ni Mama na baba walimfundisha nyumbani kusoma na unabii naye akajitambua kuwa Ndiye Masihi aliyeahidiwa. Mariamu na Yusufu walitoka koo ya kifalme, na kama isingekuwa kule kuchukuliwa Babeli utumwani wangekuwa katika ufalme, ila mambo yalibadilika wakawa watu wa kawaida.

Wengi hawakuwa na Biblia siku zile, ila walihudhuria kwenye Sinagogi, mara mbili kwa juma. Yalikuwa maisha ya ajabu ambayo tungependa kuyajua kwa undani; pale Yusufu na Mariamu walipomtunza Mwana wa Mungu. Tungetamani kujua watoto aliocheza nao, na michezo waliyocheza pia. Siku zile watoto wa kiume walikariri Agano la Kale lote, yaani Torati au vitabu vya Musa, manabii na Zaburi. Maandiko

yaliandikwa kwenye gombo refu, kama mkeka hivi, unaokunjwa na kukunjuliwa. Wazazi wake Yesu walikuwa wakienda Yerusalemu kila mwaka kama Wayahudi wote, kushiriki sikukuu ya Pasaka, Makambi na Pentekoste kwenye hekalu la Mlima Moraya, lililokuwa umbali wa mwendo wa siku chache kwa miguu. Yesu alipopata umri wa miaka 12, ambayo ilikuwa inamvusha mtoto na kumpeleka kwenye daraja la kijana au mwanamume katika utamaduni ule, naye alipanda kama ilivyokuwa desturi kwa Pasaka. Walisafiri kwa makundi kama njia ya kujihakikishia usalama dhidi ya wanyanganyi. Katika matembezi yao walizungumza maana ya siku kuu hii na jinsi walivyotoka kule Misri kwa kupaka damu ya mwana-kondoo kwenye kizingiti cha mlango, na jinsi tukio hilo linavyohusiana na Masihi Mwana-Kondoo halisi wa pasaka. Zaburi 120 hadi 134 ndizo ziliimbwa wakati wanapanda milima kuelekea Yerusalemu, zitazame na ziimbe!

Yesu alianza kuelewa kwamba Yeye Ndiye Mwana-Kondoo Yule atakayechukua dhambi za ulimwengu, akaanza kuelewa zaidi misheni yake. Walipomaliza siku kuu, Mariamu na Yusufu walirudi kwao, wakidhani Yesu Yuko nao kwenye msafara. Kumbe Yesu alikuwa amebaki nyuma huko Yerusalemu. Pengine alikuwa na wenzake wa rika Lake, waliokuwa ndugu au marafiki walifikiria, maana hili ni jambo la kawaida kwenye jumuiya ya waumini, watoto wa umri wa miaka 12 hasa enzi zile walitembea na kuzungumza na wengine kwenye msafara.

Ingekuwa enzi hizi ambazo watu hupanda mabasi pamoja huenda wasingepotezana maana ingekuwa rahisi kujua nani hajapanda. Pilika pilika za kubeba mizigo, kulisha mifugo, kuagana na kuzungumza na marafiki ziliwafanya kutotambua kama Yesu Hayupo miongoni mwao. Mama na baba wakamsahau, wakaendelea kutembea huku wakirudi nyumbani. Baada ya kutambua kuwa Yesu hayupo nao, walienda siku nzima wakimtafuta kwa jamaa na jirani zao, walipomkosa waliamua warudi Yerusalemu huku wakimtafuta njiani kote. Walihofu pengine mtoto atakuwa hatarini, ama ametekwa na watu wenye nia mbaya ya kumdhuru, kama wafanyavyo siku hizi. Ilikuwa mwendo mrefu kufika walikopiga kambi, hivyo huenda walikuwa wanapumzika njiani. Walichukua muda wa siku tatu kumpata Yesu. Wazazi walikuwa na hofu, kwamba mtoto waliyekabidhiwa kutoka mbinguni wameshindwa kumtunza. Wazazi wa Yesu walifikiria huenda Herodi mkuu aliyetaka kumwua Yesu akiwa mtoto ametekeleza nia yake ovu kupitia kwa wasaidizi wake walio hai.

Wazazi wengi siku hizi hutangaza wanapopotelewa na watoto. Hawa wanajua jinsi wazazi wa Yesu walivyosumbuka moyoni, kwa kupotelewa na mwana wao. Lakini wazazi wengine hutelekeza watoto, na kulazimisha wajilee wenyewe. Hawa wanapaswa kuchukua tahadhari maana watoto hawa tumepewa na Mungu, na siku moja atatuuliza “mtoto niliyekupa yupo wapi?” Hata kama wazazi wanafanya kazi ya Mungu, wajibu na jukumu lao la kwanza la umishonari ni kwa watoto wao.

Hata siku hizi wazazi wengi huwasahau watoto wao kwa visingizio vya kuwa na shughuli nyingi na kusababisha watoto hao kujilea kupitia kwa majirani, runinga, Ipod, teknolojia au kupitia watu tunaowaweka kama vibarua. Kibaya kupita yote, watu humpoteza Yesu kwa marafiki wabaya, shughuli, masengenyo, mitandao, fasheni, tamaa za mali au mahangaiko mengine ya dunia. Wazazi tuombeane sana!

Wazazi walikuja kumgundua Yesu akiwa hekaluni, ameketi katikati ya madaktari wa theolojia au walimu wakuu wa dini au marabi, akiwasikiliza na kuwauliza maswali. Nao wote waliomsikia, walishangaa yale aliyoyafahamu na majibu aliyoyatoa kwa maswali aliyoulizwa. Walistaajabu, maana walijua hakuenda shule maarufu walizozijua. Nawe pia leo waweza usiende shule mashuhuri za taifa, ila ukimweka Yesu mbele, uko tayari katika 'shule za kimataifa.' Alipoulizwa maswali ya Torati, Masihi na mengine alijibu vizuri mno, kwa wepesi. Walikuwa hawajawahi kuona mtoto kama huyu! Na kweli alikuwa hajawahi kuzaliwa kama YEYE!.

Wayahudi wengine walikuwa wanaenda kwenye sikukuu hizi zinazomwakilisha Masihi kama Pasaka, kama utamaduni au mapokeo tu, wakiendelea na mambo ya kila siku bila kutafakari maana ya sherehe hizo. Ila kwa Yesu siku kuu hizi zilikuwa zina maana kubwa, maana zilikuwa zinamlenga YEYE. Alipoona zile kafara zikitolewa kila siku, alianza kutambua hatua kwa hatua kile kinachowakilishwa na alama au mifano ile, na baada ya kutambua alianza kuelewa kazi iliyo mbele Yake itakayokuwa, kwa ajili ya wanadamu wote.

Alijibu maswali kwa unyenyekevu wa mtoto, akirudia Maandiko na kuleta maana ambayo walimu hawa walishangazwa nayo. Pengine hata walimwuliza, ulizaliwa wapi, Naye akajibu "Bethlehemu" na kuwafanya wajadili kama kuna unabii wa kuzaliwa Masihi katika mji huo. Mazungumzo yakawa ya furaha na matamu hata wakajisahau, na kukaa Naye siku tatu, pengine wakila Naye na kumtunza huku wakiendelea na mazungumzo. Hatujui kama siku zile tatu walilala usingizi au waliendelea na mazungumzo mpaka kukacha! Endapo viongozi hawa wa dini wangeyatilia maanani Maneno ya 'mtoto huyu', basi alipoanza huduma Yake ingekuwa rahisi kwao kumpokea kama Mwokozi na Masihi wao.

Wazazi walishangaa walipomwona Yesu hekaluni akiwa amezungukwa na watu, na mama Yake akaenda karibu Naye na kumwambia "Mwanangu mbona umetutenda hivi? Tazama baba yako nami tumekuwa tukikutafuta kwa huzuni tukifiri umepotea." Yesu alijibu "Kwa nini mnanitafuta, hamkujua kwamba inanipasa kuwa katika nyumba ya Baba yangu?" ili nijifunze anachotaka nifanye. Wazazi hawa walitatizwa na kauli Yake, wakafikiri mengi "Kama anamwita Mungu Babaye, pengine hivi karibuni ataenda kwa Baba Yake na kutuacha" au "mbona mtoto huyu anatudhalilisha mbele ya watu wakati sisi ndiyo wazazi Wake tunaomlisha na kumvisha." Ila baada ya kufufuka Kwake walielewa haya yote kwa undani, japo mara moja moja shaka iliwaingia tena.

Hata leo Kanisa ni nyumba ya BWANA. Yesu alifurahi kudumu kanisani. Tusipige chenga kwenda kanisani, au tusijicheleweshe kufika kanisani, na tuingiapo kanisani tusifanye michezo. Watoto wa miaka 12 wanajifunza mambo mazito ya ubongo mwingi mashuleni leo hii, basi kanisani tusifikiri watoto hawa hawana uwezo wa kuelewa Maneno ya Mungu. Mara zingine watu wamefikiri wakikaa nyumbani watapata maarifa ya Neno la Mungu zaidi, hii si kweli, chuma hunoa chuma; na mara nyingi tukikaa nyumbani tunakosa mfariji na kuingia uvivu. Mara zingine watu huja kututembelea siku ile tunayoacha kwenda kanisani na matokeo yake tunaacha maombi na mwishowe tunanza kuingilia mambo mengine kama kugombana

gombana, kupika, kuangalia mifugo au kufagia.

Mtoto wa Mungu anapaswa kupenda kuwa kwenye nyumba ya BWANA. Kusoma Maandiko ya Mungu ni shughuli ya Baba yetu iliyo muhimu kupita zote. Wazazi hawakuelewa Yesu anachokisema; maana iliwachukua muda kutambua kuwa Baba Yake ni Mungu. Walifikiri pengine Baba yake atamchukua karibuni! Na marabi huenda walijiuliza 'tulidhani Baba Yake Yuko mbinguni, na huyu aliyekuja kumchukua yeye ni nani? Basi Wakarudi kwao Nazareti, na Yesu kwa kuwa alikuwa Mungu alijawa na hekima ya mbingu kupita miaka Yake, na neema ya Mungu ilikuwa Naye, na aliendelea kuwatii wazazi Wake. Mama yake akaweka hayo moyoni mwake.

*Maombi yanahitajika kuwa na misimamo isiyo maarufu au isiyopendwa -Inahitaji ujasiri wa kimaadili, uthabiti, kuazimia, uvumilivu, na maombi mengi kukaa katika upande ule tofauti usiopendwa na wengi. Tunashukuru kwamba tunaweza kuja kwa Kristo kama wale maskini wanaoteseka walivyomjia Kristo hekaluni.

--------------------------------------

Maswali: Simeoni alisema maneno gani? Ana alikuwa nani? Kwa nini watu wengine hawakujua Masihi amezaliwa? Mariamu alimwambiaje Yesu alipompata baada ya siku tatu? Yesu alijibuje? Kwa nini Yesu alitii wazazi Wake?

**SIKU YA 198.**
**(Julai 16)**

# Utoto wa Yesu na Yohana mbatizaji.

**Luka 3, Mathayo 3 na Marko 1.**



Biblia iko kimya kuhusu maisha ya Yesu utotoni. Mtu angepata kurasa tano na picha angalau moja ya Yesu utotoni, angeiuza kwa mamilioni ya pesa leo! Mungu kwa hekima yake aliamua habari zake za utotoni zisiandikwe. Wengi wameongeza maneno yao, ila Biblia ipo kimya. Ila twaambiwa alitii wazazi Wake, akimsaidia babaye katika kazi ya useremala, na mamaye katika kazi za nyumbani. Kama watoto wengi siku zile alirithi kazi ya useremala ya baba Yake Yusufu, hata baba alipokufa alimsaidia mama kwa kupata riziki. Mariamu alimfundisha Yesu Maandiko siku kwa siku. Walipitia unabii wa Masihi na kazi atakayofanya.

Mama huyu alitenga muda wa kumwonyesha mtoto mimea, maua, na wanyama ambao Yeye Mwenyewe aliumba miaka maelfu iliyopita. Lazima atakuwa mtoto ambaye wazazi walimfurahia mno, maana alitii, na hakufanya dhambi. Hakubishana pale wazazi walipomtuma, au walipomwambia kufanya jambo fulani. Alikuwa mtoto anayependeka. Alikua kiroho, kimwili, kijamii, na kiakili, akifikiria wengine bila kuwa mbinafsi. Alikuwa mpole na Mwenye huruma. Aliishi kubariki wengine japo alikuwa na mapambano makali dhidi ya nguvu za giza, kwa maana Shetani alitaka kumtega na kummaliza.

Aliishi maisha rahisi ya kuchapa kazi, na wala hakukaa kivivu, hali iliyomsaidia kukaa salama dhidi ya majaribu ya mwovu maana akili ya mtu mvivu ni karakana ya Shetani. Hakutumia Uungu Wake kuyafanya maisha kuwa rahisi. Maana hakushuka toka msalabani na kukimbia! La! Hasha! Jambo hili linatufundisha sisi watoto kuwa watenda kazi bora. Hauhitaji talanta kubwa ya kufanya kazi nzuri. Mtoto wahitaji nidhamu ya kupenda kazi ngumu. Yesu aliishi na watu masikini maisha Yake yote na Yeye Mwenyewe alikuwa masikini, ila alijali masikini na matajiri pia.
Maisha ya utulivu, na rahisi ni muhimu. Maisha ya kelele mijini yafanya mtoto awe na mihemuko, hofu, mashaka au tabia mbaya. Wengi tunastaajabu maisha ya Yesu ya miaka mitatu na nusu, ila msingi wake ni ile miaka 30 aliyoishi nyumbani. Ule utoto wa Yesu ndiyo uliyomfanya awe alivyo alipokuwa mtu mzima. Alijifunza kuwa mvumilivu. Hakujitenga mbali na watu au kuwa kuishi maisha ya utawa ya kujifungia kwenye kituo cha kiroho. Alikuwa tayari kuhudumia wengine, jambo ambalo liliwachukiza wengi, maana tabia yake iliwashitaki. Hata hivyo watu wengi walipenda kuwa karibu Naye, maana hakuwa anataka kupigania haki Zake, au kupigana na wenzake.

Yesu aliendelea kujifunza kuhusu Yeye kama binadamu na kama Mungu. Hili haliwezi kuelezeka kwa ulimi wa kibinadamu. Akawasiliana na Baba Yake wa mbinguni kuhusu mawazo, maarifa na hisia Zake. Lengo Lake likiwa kutimiza kazi ambayo Mungu alikuwa amempa. Aliepuka yote maovu kama kunywa pombe, uvivu, uongo na yale matunda ya uovu ya Wagalatia tano. Alipanga ni muda gani atafanya kazi ya useremala, na ni wakati gani ataanza kuhubiri; na kila alichofanya alikifanya kwa ufanisi na furaha zote. Kazi inasaidia kutayarisha tabia za watoto na wakubwa, ili wafike mbinguni. Mariamu alikuwa mara nyingi akitafakari juu ya kuzaliwa Kwake na yote aliyoshuhudia, akajiuliza moyoni kama hii ilikuwa ni ndoto au ni kweli.

Katika mwaka wa 15 wa Kaisari Tiberio, wakati kuhani mstaafu Anasi na kuhani Kayafa walikuwa makuhani, Neno la Mungu lilimfikia siku zile Yohana, akafika nchi yote iliyokuwa kando na mto Yordani akihubiri watu ubatizo wa toba iletayo ondoleo la dhambi. Kama ilivyoandikwa na nabii Malaki “sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya BWANA, yanyosheni mapito Yake. Kila bonde litajazwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; palipotoboka patakuwa pamenyoka. Na palipoparuza patalainishwa; na wote wenye mwili watauona utukufu wa Mungu.”
Ndivyo alivyopata jina la Yohana mbatizaji. Yohana mbatizaji alizaliwa kwa kusudi maalumu la kutayarisha njia kwa ajili ya Masihi, ili watu watubu dhambi zao na kujitoa mioyo yao kwa Mungu ili wapokee wokovu ambao Yesu ametoa. Yohana aliishi maisha ya kujikana nafsi, na nidhamu. Hakula chakula chochote tu alichokipata, kwani alikuwa mnadhiri wa Mungu. Hakunywa pombe au kileo chochote. Chakula chake kilikuwa cha asili, si kama vile ambavyo binadamu tumejitungia leo.

Hata leo nasi tunapaswa tuishi maisha rahisi ya kujikana nafsi tangu utotoni, kama Yohana mbatizaji. Tupatapo chakula tuepuke kukifanyia ufundi unaopunguza thamani yake. Maisha ya utotoni ya Yohana Mbatizaji ndiyo yalimtayarisha na kumfanya awe vile alivyo, na kuhudumia watu kwa namna alivyohudumu. Ubatizo aliowapa watu ulikuwa wa toba na unaotayarisha mioyo, ili Masihi akija wawe

tayari. Hata leo watoto na wakubwa wote tunapaswa kutayarisha watu kumlaki Yesu mawinguni, yaani majilio au ujio wa Yesu wa pili.

Yohana mbatizaji ni mfano wetu sisi tunaomngojea Yesu na ambao tunatakiwa pia kutayarisha watu. Twapasa tujikane nafsi na kuishi maisha rahisi, ili tuweze kupeleka ujumbe kwa watu. Yohana ambaye baba yake alikuwa kuhani angepaswa kuwa kuhani pia, ila elimu hiyo ya ukuhani uliokuwepo siku zile isingemsaidia kufanya kazi Mungu aliyotaka aifanye. Mungu alimchukua nyikani ajifunze toka kwake mwenyewe. Huko nyikani kusikokuwa na makelele, akajifunza Maandiko na mambo mengine kutoka kitabu cha Mungu cha uumbaji au mambo ya asili. Maisha ya mijini mara nyingi kwa watoto yanaondoa utulivu wa kujifunza mambo ya kiroho au kujenga tabia njema. Kujikana nafsi na kuwa na kiasi ni muhimu kama tunataka kuwa wafuasi Wake Bwana. Mungu alifanya maisha ya hawa binamu wawili yasikutane!

Kutokana na ule unabii wa Danieli 9 mwaka huu wa 15 wa kutawala Kaisari Tiberio ndiyo ule wakati wa Masihi kupakwa mafuta. Mungu ni wa ajabu, alitabiri haya zaidi ya miaka 600 iliyopita. Rudi na kuangalia unabii huu wa Danieli tisa. Mamaye Yohana mbatizaji, alikuwa binamu wa Mariamu mama wa Yesu, japo vijana hawa wawili, walikuwa hawajaonana toka wazaliwe, kwa maana waliishi mbali mbali. Yohana alipelekwa nyikani, mbali na mijini, ili tabia yake itayarishwe kwa kazi hii kubwa. Alipofika kando ya mto Yordani, kuanza kazi alihubiri bila kuwapaka watu mafuta kwa mgongo wa chupa. Alisema wazi wazi "Tubuni, maana ufalme wa Mbinguni umekaribia."

Yohana mbatizaji, ni nabii aliyenenwa na nabii Malaki akifananishwa na Eliya, ya kwamba atakuwa mtayarishaji njia ya Masihi. Huenda Mariamu alizungumza na Yesu kuhusu undugu wao na Yohana na kile anachohubiri kuhusu kutayarisha njia ya Yesu! Walizungumza kuhusu ubatizo, na jinsi watu wanavyokwenda mtoni Yordani.

*Maombi Yanayohitajika ili Kuingia Mbinguni — Hakuna kitu kama kuingia kwetu kwenye malango ya mbinguni kupitia kujifurahisha, kujiendekeza na upumbavu, maburudisho, ubinafsi, bali tu ni kwa kukesha na kuomba bila kukoma. Kukesha kiroho kwa kila mmoja wetu ndiyo gharama ya usalama. Usiegemee upande wa Shetani hata sentimita moja, asije akapata manufaa kwako na kukuteka

---------------------------------------------

Maswali: Biblia yasema nini kuhusu utoto wa Yesu? Yesu alifanya kazi gani kupata riziki nyumbani kwao? Kwa nini kazi ni muhimu kwa kila mtoto? Kwa nini Yohana mbatizaji aliishi nyikani na kula vyakula rahisi? Yohana mbatizaji alisema nini kwenye mahubiri yake?

**SIKU YA 199.**
**(Julai 17)**

# Yesu Asimikwa kwa Ubatizo mto Yordani.

**Yohana 3, Marko 1. Luka 3**



Ndipo siku moja Yesu aliaga familia Yake, wakakumbatiana wakiagana, na mamaye. Yesu akiwa Mwana mwema lazima alifanya mipango ya kumwacha mama Yake vizuri, maana yaonekana Yusufu alikuwa ameshaaga dunia. Wakati ulikuwa umefika! Wakati uliotabiriwa toka kuwekwa misingi ya dunia. Je, aghairi kuingia kwenye kazi iliyomleta ili akimbie msalaba? La! Yesu aliendा mbele hakurudi nyuma kinyume cha mpango ule. Yohana alikuwa na miaka 30 alipoanza hii huduma, na Yesu alikuwa ana miaka 30 pia, ila Yohana alikuwa mkubwa kwa Yesu kwa miezi 6; walikuwa ni binamu ambao hawajawahi kukutana.

Siku zile watu wakaambiana nabii ameinuka na anahubiri, akiwapa watu maneno ya Mungu. Ilikuwa imepita miaka 400 ya ukimya bila nabii yoyote, tangu nabii wa mwisho wa Agano la Kale alipomalizia, na watu wakafurika kumsikia, maana walisikia siyo kwamba anasoma Maandiko tu bali anawaambia watu kile Mungu anachomjulisha moja kwa moja. Aliwaambia wasiwe na kiburi cha matendo yao mazuri, au dini yao, kwani Mungu ana uwezo wa kuinua waumini wazuri kutoka kwenye mawe, na wala hahitaji uzao wa Ibrahimu. Toba ya kweli ni kujutia dhambi, kuungama kwa Mungu na watu ambao tumewatendea mabaya. Watu hawakukasirika walipoambiwa hivyo, hata Herodi pia aliambiwa ukweli.

Pambano kubwa ni kujikana nafsi na kutojifikiria bali kufikiria wengine na Mungu. Kujitoa kikamilifu kwa Mungu na kuacha njia mbaya, au mapenzi yetu ndiyo siri ya kuwa mtu wa Mungu. Tusifikirie kuwa wale wengine ndiyo mabaya zaidi yetu, bali tujihoji makosa yetu na kuyatubia. Yohana bin Zakaria, hakuvaa kama watu wa kawaida, bali kama manabii wa zamani. Alivaa vazi la singa za ngamia na mshipi wa ngozi kiunoni mwake, na chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwituni.
Watu wote wa Yerusalemu, Uyahudi na nchi zote kando ya Yordani wakamwendea, naye akawabatiza katika mto Yordani, huku wakiziungama dhambi zao. Yohana alitaka kuwa penye maji mengi, ili abatize watu. Ubatizo ni neno la Kiyunani lenye kumaanisha kuzamishwa majini. Yohana akaona mafarisayo na masadukayo wengi wakiujia ubatizo. Haya yalikuwa makundi ya uongozi wa dini na siasa, yaliyoamini mambo yanayotofautiana. Mafarisayo waliamini kuwepo kwa malaika, ufufuo na Maandiko yote.

Masadukayo wao hawakuamini malaika wala ufufuo. Kuwa msadukayo, ni kutokuwa na imani kabisa ya Mungu wa mbinguni, maana bila ufufuo, hakuna tumaini, au kumwamini Yesu aliyefufuka. Mafarisayo walijua Maandiko yote kuliko kila mtu, ila hawakufanya yale waliyojua, bali walijiongezea sheria nyingi na kufanya kumcha Mungu kuwa mzigo au kongwa. Basi Yohana alipoona makundi haya mawili, aliwaambia "Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya nyinyi kukimbia hasira inayokuja? Basi zaeni matunda yapasayo toba." Yaani waungame na kutenda mema, wala wasiwaze mioyoni mwao kuwa wanaye baba Ibrahimu, na huku matendo yao ni maovu, kwani Mungu aweza kumwinulia watoto Ibrahimu hata kutoka kwenye mawe."

Leo tungesema tusiwe na kiburi kwamba sisi ni wa muhimu kwa vile dhehebu letu ni hivi au vile kwani Mungu aweza kuinua waumini wazuri hata kutoka kwenye mawe. Mhubiri huyu mashuhuri aliyekuwa kwenye taarifa za habari zote akasema "Shoka limekwisha kuwekwa kwenye mashina ya miti, na kila mti usiozaa matunda mazuri, hukatwa na kutupwa motoni." Yaani wale wenye uovu na matendo mabaya watapata hukumu na adhabu wasipate uzima wa milele.

Wengine waliangalia yatakayotokea, na mahubiri ya Yohana yalivyokuwa ya ajabu na kukatisha watu shauri kuacha uovu, wakawaza mioyoni mwao kwamba pengine Yohana ni Masihi. Bali Yohana akawaambia anawabatiza kwa maji tu, ili watubu, ila anayekuja nyuma yake Ndiye Masihi, huyo atakuwa na nguvu kuliko yeye Naye atawabatiza kwa moto au Roho Mtakatifu. Akawaambia yeye hastahili hata kufungua viatu vyake kamba, au kuwa hata mtumishi wake, maana ni mkuu sana. Aliwaambia kuwa Masihi atakapokuja, "Huyo atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto. Pepeto Lake li mkononi na atasafisha shamba lote, na kukusanya ngano ghalani, bali makapi au wale wasio na matendo mema watateketezwa kwa moto."
Wakati huo Yesu akaja toka Galilaya kwao, mpaka Yordani akiwa na miaka 30 ili abatizwe na Yohana. Yesu alimjua Yohana toka zamani! Japo alikuwa hajawahi kumwona maana Yesu alikuwa mbinguni wakati baba yake Yohana akijulishwa na malaika kuzaliwa kwa Yohana! Yohana alipomwona Yesu aja, japo walikuwa hawajaonana Roho wa Mungu alimwonyesha "Huyu Ndiye Masihi"; Yohana akastuka, na akataka kumzuia Yesu akisema "Mimi nahitaji kubatizwa na Wewe,

Nawe waja kwangu?" Yesu akamwambia "Kubali hivi sasa, kwa kuwa inatupasa kuitimiza haki yote."

Yesu hakuhitaji kubatizwa, ila alibatizwa atupe mfano tunaotakiwa kuufuata, na ndipo Yohana akakubali na kumbatiza. Wengi siku hizi hubatizwa wakiwa na umri wa miaka kumi, na hili laweza kuwa sawa kama mtoto huyu amefundishwa na kuelewa wokovu. Yesu alisema ni sawa, ikiwa watajifunza na kuelewa basi wabatizwe kwa Jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Yesu alipomaliza kubatizwa, alipanda toka majini na kupiga magoti akiomba; na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kwa umbo la hua, akija juu Yake; na Tazama sauti kutoka mbinguni ya Mungu Baba ikasema "Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye."

Kubatizwa kwa Yesu ndiyo kupakwa Kwake mafuta kuanza kazi yake ya Masihi. Hata leo tunapobatizwa ni muhimu tuombe Roho Mtakatifu. Ubatizo ni kuacha maisha ya zamani na kuingia maisha mapya, na Yesu. Ni kuiambia dunia hadharani kwamba wewe sasa ni wa Mungu. Zamani Wayahudi walikuwa na tohara iliyosimama mahali pa ubatizo, ila siku hizi tuna ubatizo wa maji na Roho. Tunaachana na maisha ya zamani, huku mioyo na mawazo yetu ikijazwa Roho Mtakatifu, anayetuwezesha kutembea na kushirikiana naye. Biblia inasema ni kufa katika matendo ya zamani, au kuyaacha mambo ya kale ya uovu.

BWANA ni Mmoja, ubatizo ni mmoja na imani ni moja tu. Ubatizo wa Yesu ulikuwa tangazo la rasmi kwamba Masihi amewadia na huduma Yake imeanza. Hakuwa na haja ya kubatizwa kwa vile hakuwa na dhambi, ila alibatizwa ili kutupa sisi mfano. Alianza huduma Yake kwa wadhambi waliokuja kubatizwa Yordani, na akaishia huduma yake kati ya wadhambi au wezi wawili waliotundikwa msalabani. Ujumbe wa Yohana ni wetu pia, haijalishi kama dhambi zetu ni za kiburi, kutotii au kuvunja sheria (uhalifu) twahitaji tubatizwe, na kuacha dhambi na kuanza maisha mapya. Kusikitika kwamba tumekosa haitoshi, twahitaji kutubu na kuwa na uhusiano Naye. Yesu hakuwa na haja ya kubatizwa ila alituwekea mfano sisi, na kutimiza Maandiko. *Maombi yanatufanya kudumu kuwa Waaminifu — Bila maombi yasiyokoma na kukesha kwa bidii, tuko katika hatari ya kuongeza uzembe, kutojali na kupotoka mbali na njia sahihi. Adui daima anatafuta kuzuia au kufunga njia ya kukifikia Kiti cha Rehema, ili kwa sala ya dhati na imani tusipate neema na nguvu ya kupinga majaribu.

--------------------------------

Maswali: Yesu alipobatizwa ni nini kilitokea? Yohana alikula na kuvaa nini? Kuna ubatizo wa aina ngapi? Ubatizo maana yake ni nini? Ni wakati gani mtu hubatizwa? Yohana alijuaje huyu ni Masihi? Kwa nini Yohana alisita kumbatiza Yesu? Sauti toka mbinguni ilisemaje? Kwa nini ni vizuri tujue Mungu au Roho Mtakatifu hajaribu bali Shetani ndiye anayetujaribu?

**SIKU YA 200.**
**(Julai 18)**

# Yesu anajaribiwa na Shetani nyikani.

**Luka 4, Mathayo 4.**



Watu walikuwa wakibatizwa, wakiwa na nia ya kubadilika na kufuata njia ya Mungu. Walielewa ni nini kinaendelea, na ujumbe uliozungumzwa ulikuwa ukichoma mioyo yao. Walimwuliza Yohana mbatizaji "Tufanye nini basi?" Naye akawajibu wawe na huruma; mwenye nguo mbili, na ampe asiye na nguo, na mwenye vyakula amsaidie mwenye njaa. Na watoza ushuru nao walikuja wakauliza "mwalimu tufanye nini?" Naye akawaambia "wasitoze kitu zaidi ya ilivyoamriwa" au isivyokuwa halali yao. Askari nao walikuja wakauliza "sisi nasi tufanye nini." Hawa aliwaambia "wasiwe wakatili na kumdhulumu mtu, wala msimshitaki mtu kwa uongo, bali mtoshewe na mishahara yenu."

Hata leo twangoja ujio wa Yesu mawinguni mara ya pili. Hatuwezi kuwa kimya. Lazima tuwaambie watu wajitayarishe ili wapate uzima wa milele kwa njia ya kusaidia wenye mahitaji na waondokane na tamaa ya fedha, maana shina la maovu yote ni kupenda pesa. Kunung'unika wakati Mungu ametubariki, au kuona wivu kwa kuwa mtu fulani ametuzidi hiyo nayo ni dhambi. Utauwa na kuridhika ni faida kubwa. Yohana alihubiri watu kwa maonyo mengine mengi. Alimkaripia mfalme Herode ambaye alikuwa wa mbari yake, kwa ajili ya kumchukua mke wa kaka yake Herodia. Jambo hilo lilimkasirisha Herode akaamua kumfunga Yohana mbatizaji gerezani.

Yesu alipobatizwa, baada ya Roho Mtakatifu kushuka alirudi kutoka Yordani akiongozwa na Roho kwa muda wa siku 40 nyikani, mahali kusipokuwa na watu wala maduka; akifunga bila kula kitu usiku na mchana. Alitafakari na kupanga kazi ya wokovu wa mwanadamu. Kufunga ni muhimu, kuanzia umri fulani, kama huna tatizo la afya; kisukari au vidonda vya tumbo. Unaachia mlo mmoja au miwili kwa siku. Watu wengi wakiacha kula siku moja tu wanapata njaa sana. Hatushauri mtoto wa kawaida wa miaka 12 hivi afunge zaidi ya siku, ila wapunguze milo!
Watu wazima ndiyo wanastahili kufunga siku 40 wakinywa juisi za matunda na mboga na maji. Maji ni muhimu hata unapofunga, maana yana namna ya kusafisha mwili. Inapendekezwa wakati wa kufunga watu wasile chakula usiku, maana ni

madhara kwa mwili mtu anapolala na chakula kikiwa kimejaa tumboni. Wengine waliowezeshwa na Roho wa Mungu kufunga siku 40 walikuwa Eliya, Paulo na Musa. Ikawa Yesu alipofikia mwisho wa siku Zake za kufunga au kutokula kitu alisikia njaa na udhaifu na hapo ndiyo akamwona Ibilisi akija kumjaribu na kumwamrisha kama vile anavyotufanyia sisi wanadamu katika mawazo yetu kila siku, tofauti ni kuwa hapa Shetani alikuwa katika hali ya mwili.

Hakika Mungu ni Upendo, kwani alikubali Mwana Wake aje kwenye mapigano makali ambayo kila binadamu anakabiliana nayo, na kupigana kila siku. Yesu alikuwa na hatari ya kushindwa na kupoteza uzima wa Milele kama sisi, kama asingejua alikotoka, kazi Yake na wajibu Wake na Yeye ni nani. Sisi tunaingia katika hatari ya kushindwa na kupoteza uzima wa milele tunaposhindwa kujielewa kwamba sisi ni taifa takatifu, ukuhani wa kifalme watu wa miliki ya Mungu tulioitwa kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyetuita tutoke gizani na kuingia katika nuru Yake ya ajabu. Tukisahau hayo tunarudi kwenye giza na tunapoteza uzima wa milele.

Yesu alimfahamu kiumbe huyu aliyeumbwa kama Lusifa au nyota ya asubuhi, aliyeishi mbinguni pamoja naye kwa miaka mingi. Shetani ana sura nzuri tu ya kupendeza, lakini wengi wamemchora mwenye mapembe na sura ya kutisha. Shetani aliumbwa na sura nzuri kweli kweli na wengi wasingemfuata kama angekuwa na sura mbaya tunayoona kwenye magazeti leo. Shetani akafunua mdomo wake na kusema "ukiwa Ndiwe mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate."
Hili si jaribu letu sisi, maana hata tungekaa siku nzima kwenye mawe mengi tusingeyabadilisha kuwa mikate. Ila Yesu angeweza kufanya hivi kirahisi sana, na wala mtu asingejua amefanyaje. Yeye alijua kwamba uwezo Wake wa Kiungu ulikuwa si kwa manufaa Yake bali kwa nia ya kuwasaidia wengine kwani twaona baada ya muda kidogo akilisha zaidi ya watu 5,000. Hata hivyo Yeye alikuwa Mungu tayari, na hakuhitaji kumhakikishia mtu au Shetani jambo hilo. Hakuwa na haja ya kutii amri za Shetani. Yesu akamwambia "Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Kisha Ibilisi yaani Shetani akamchukua Yesu mpaka mji mtakatifu Yerusalemu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, kisha akamwamuru "Ukiwa Ndiwe mwana wa Mungu jitupe chini, kwa maana imeandikwa kwenye Zaburi 'atakuagizia malaika Zake, Na mikononi mwao watakuchukua; usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe." Shetani anajua Maandiko na ana uwezo wa kuyanukuu kuliko mwanadamu kwani ana uzoefu wa zaidi ya miaka 6000 kazini. Hapa alinukuu kitabu cha Zaburi 91, ila alitumia ujumbe huo nje ya muktadha, akiyapindisha maneno ili yamfae yeye. Na kila wakati Yesu aliponukuu Maandiko na yeye alimfuatiliza Yesu akijidai kusema "imeandikwa" huku akiyapotosha tafsiri yake.

Jambo la kukumbuka ni kuwa Shetani anajua Maandiko kuliko wewe na aweza kutoa watu jasho na mafungu ya Biblia. Kujua kwetu Maandiko, hakusaidii kama mioyo yetu haibadiliki na  kumtii Yesu. Yesu alijua jambo lililotakiwa na Shetani si mapenzi ya Mungu kwani hakuna haja mtu ajitie hatarini bila sababu ya maana. Yesu alikuja kuokoa watu kwa kutumia upendo na si kwa njia ya mazingaombwe au sarakasi. Basi Yesu akamwambia tena "Imeandikwa usimjaribu BWANA Mungu

wako." Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno pengine ni zaidi ya mlima Kilimanjaro, akamwonyesha milki zote zote za ulimwengu; nchi mbali mbali kama Tanzania, Burundi, Kenya, Rwanda, Marekani, Chile, Japani, Australia, Kongo au Uganda na fahari yake, akamwambia, haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia "Nenda zako, Shetani, kwa maana imeandikwa, msujudie BWANA Mungu wako, umwabudu Yeye peke Yake." Hapa tunajifunza kwamba hata sisi tukijitoa kikamilifu kwa Mungu leo, twaweza kumfukuza Shetani atoke, na kumpinga, naye atatimua mbio. Shetani ana nguvu nyingi kuliko sisi, kama tutasimama wenyewe, hivyo tunashauriwa kusimama nyuma ya Yesu. Kisha Ibilisi akamwacha, akijua ameshindwa kwa vile Yesu alitumia Maandiko na hivyo hakusikiliza maneno ya Ibilisi.

"Imeandikwa", ndiyo salama yetu na kimbilio letu hata leo. Maovu mengine tutayashinda kwa sababu tunajua kweli na uongo, tutajua tu kwamba huu ni uongo wa Ibilisi. Yatupasa tuweke Neno la Mungu mioyoni mwetu, hapo tutakuwa na uwezo wa kusema "imeandikwa." Hatuwezi tukasema imeandikwa, bila kujua ni nini kimeandikwa!. Majaribu yetu siku hizi yanakuja kwa njia zile zile pia; kupitia majaribu ya chakula, mamlaka na dhana potofu. Tunajaribiwa na mwovu na si Mungu. Jaribu letu kubwa ni kujaribu kujitegemea wenyewe, na kuacha kutegemea uwezo wa Mungu.

Shetani anataka tupoteze uzima wa milele maana yeye alipoteza mbingu. Kazi yake masaa 24 kwa wiki nzima ni kutaka tuangamie. Aliwasababisha Wayahudi wasiwe na nafasi na shughuli za kutoa kafara na kupoteza thamani ya vile vielelezo vya Masihi anayekuja.
Yesu alizaliwa na udhaifu wa kibinadamu, ila alishinda vishawishi bila kumwasi Mungu. Yeye alikuwa na majaribu yaliyokuwa magumu zaidi kuliko yetu lakini alishinda. Kwa kushinda Kwake majaribu ameandaa njia ili sisi pia tushinde na kisha tupone. Mara nyingine twaweza kupata jaribu la kupoteza marafiki, kupoteza kazi, au mambo mengine, lakini kama Wakristo tunaompenda Mungu, lazima tushinde hali hiyo kwa kumwambia Shetani "imeandikwa."

Maandiko yanatuonya tusimjaribu Mungu. Ni sehemu moja tu katika kitabu cha Malaki sura ya tatu tunapoambiwa tumjaribu Mungu. Basi unapojaribiwa leo, kumbuka kimbilio lako ni "imeandikwa" na kisha mwombe Mungu akusaidie kutenda yale "yaliyoandikwa." Kutawala tamaa zetu za chakula, na tamaa zingine ni jambo la muhimu sana. Majaribu mengi yajayo kwa njia hizo yameangusha wanadamu wengi. Wale tunaopambana na ulafi au tamaa zingine za mwili tuna jambo la kujifunza hapa. Kila ahadi ambayo Mungu ameiweka kwenye Maandiko Yake, ni silaha yetu ambayo kwa kuinukuu twaweza kuitumia kumshinda mwovu. Shetani hawezi kutulazimisha kufanya uovu, kama tutajitoa Kwake kikamilifu. Majaribu yanatuimarisha tuwe na nguvu zaidi, na kuwa waaminifu Kwake.

Yesu alikuwa na njaa malaika wa mbinguni wakaja wakamtumikia kwa kumfariji na kumpa chakula. Yesu akarudi kwa nguvu za Roho, akaenda Galilaya; habari zake zikaenea katika nchi zote za kandokando. Naye akafundisha katika masinagogi yao, akitukuzwa na watu wote. Biblia yasema Shetani alitoka akamwacha Yesu kwa

'muda' tu baada ya jaribu la tatu, ikimaanisha aliendelea kumfuata maisha yake yote, ila Yesu alishinda katika majaribu yote.

*Omba kwa ajili ya Roho- Ikiwa tunataka kujifunza juu ya Kristo, lazima tuombe kama vile ambavyo mitume waliomba Roho Mtakatifu alipomwagwa juu yao. Tunahitaji ubatizo wa Roho wa MUNGU. Hatuko salama hata kwa saa moja tunaposhindwa kutoa utii kwa Neno la MUNGU.
-----------------------------

Maswali: Ni watu gani walimwuliza Yohana Mbatizaji Maswali? Je Yesu alikuwaje tofauti na wanadamu wengine? Majaribu matatu ya Yesu yalikuwa yapi? Yesu alijibuje? Somo hili linakufundisha nini? Je ukijaribiwa wapaswa kufanya nini? Roho Mtakatifu alionekana kwa jinsi gani kwenye ubatizo wa Yesu?

**SIKU YA 201**
**(Julai 19)**

# Kuita wanafunzi wa kwanza

**Yohana 1.**



Yesu alipotoka kufunga siku 40 na kushinda majaribu ya mwovu, alirudi kwa binamu yake Yohana mbatizaji kule Yordani. Alijichanganya na watu na hakutenda miujiza pale mtoni Yordani. Yohana alikuwa nabii wa Mungu aliyetumwa ashuhudie nuru, yaani amshuhudie Yesu ili wote wapate kumwamini, maana ulimwengu wa wakati huo haukumtambua. Yesu alikuja kwao, ila walio wa Kwake hawakumpokea. Ila wale wote waliompokea zamani na leo pia, amewapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu. Si baraka kubwa hiyo? Yaani tukiliamini Jina lake, tunazaliwa tena si kwa damu na nyama bali tunazaliwa kama wana wa Mungu. Mungu alimtuma Yesu ili afanyike mwili, na kukaa kwetu ili tuone utukufu, wa Mwana pekee wa Mungu atokaye kwa BABA amejaa neema na Kweli.

Yesu alitembea akiwaambia watu "ufalme wa Mungu umekaribia." Yesu alijiepusha na watu mara nyingi ili asali, na mara nyingi alienda mahali pa faragha ili aombe. Alipenda kuomba milimani, katika bustani na penginepo palipo na faragha. Aliomba usiku kucha kabla ya kuchagua wanafunzi Wake. Basi Siku iliyofuata,

Yesu akisimama kwenye ukingo wa mto; Yohana akamsonda kidole na kushuhudia akisema kwa kupaza sauti "Huyu Ndiye niliyenena habari zake ya kwamba, ajaye nyuma yangu amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu. Kwa kuwa katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema. Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa neema na Kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo. Hakuna mtu aiyemwona Mungu wakati wowote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu Ndiye aliyemfunua."

Yohana aliendelea kushuhudia watu walipotumwa kumwuliza "Je wewe ni nani, Je Wewe ni Kristo? Je u nabii Eliya?" Alisema yeye ni "sauti ya mtu aliaye nyikani" Ili ainyoshe njia ya BWANA." Watu lazima walimtazama Yesu tena na tena na wakasogea ili kumwangalia kwa karibu. Siku iliyofuata Yohana mbatizaji akamwona Yesu akipita kwake, naye akawaambia watu tena "Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Akawaambia watu kwamba "Huyu Ndiye niliyenena" kwamba Yuaja nyuma yangu ambaye amekuwa kabla yangu. Wala mimi sikumjua; lakini kusudi adhihirishwe kwa Israeli ndiyo maana mimi nalikuja nikibatiza kwa maji. Yohana akawaambia watu ameshuhudia Roho wa Mungu akishuka kama njiwa, kutoka mbinguni, na Roho akaa juu ya Yesu.

Akawaambia watu yeye hakujua ila Mungu aliyempeleka kubatiza watu alimwambia "Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu Yake, huyo Ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu." Kama kuna Maneno yenye nguvu yalikuwa haya. Wayahudi waliyaelewa vizuri kuliko sisi, maana walikuwa wanatoa kafara ya kondoo kila siku kwenye madhabahu. Walimchinja kondoo shingoni, mishipa ya damu ikakatika, damu ikavuja, maisha ya kondoo yakaisha, kisha wakamteketeza kwa moto yule kondoo. Maneno haya ndiyo msingi wa imani yetu na injili. Bila Mwana-Kondoo wa Mungu Yesu kufa kwa ajili yetu tungekuwa bado tumepotea kwenye dhambi zetu. Twamshukuru Mungu kwa Mwana-Kondoo; maana daima mshahara wa dhambi ni mauti.

Siku ya pili yake tena Yohana akisimama na wanafunzi wake wawili, akamwona Yesu anatembea. Yohana akasema tena "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu." Watu wengine walishangaa wakimwona kijana Yesu mtu wa kutabasamu, na mwema ila hawakuona zaidi ya hilo. Wakafikiria atachukuaje dhambi za dunia huyu kijana? Ila wanafunzi walikuwa wameonyeshwa na Roho kwa vile walikuwa wamejitoa wakfu kumcha na kumwabudu Mungu. Leo hii tukisikia maneno haya tunayaona ni matamu na ya kuokoa. Hata wale wanafunzi wawili wa Yohana walipomsikia, wakamwacha mwalimu wao Yohana, wakamfuata Yesu wazungumze Naye kwa faragha.

Yesu alipogeuka na kuona wanamfuata alitaka awapime kama wanajua wanachokifanya au ni bendera ifuatayo upepo tu. Akawatupia swali kama anayetingisha kibiriti "Mnatafuta nini?" Wanafunzi walijibu "Rabi unakaa wapi?" Rabi ni mwalimu; Yesu akawaambia "Njoni nanyi mtaona." Wakaenda na kukaa Kwake siku hiyo, nayo ilikuwa yapata saa kumi na mbili. Walisikia mafundisho ya ajabu, mafundisho matamu, na ya Kweli ambayo ni halisi. Andrea na Yohana wavuvi wawili walikuwa wamekuja na kupata ubatizo wa Yohana, na wakaendelea

kutaka kujifunza zaidi. Siku ile moja ya kukaa na Yesu ilitosha kuwafungua macho yao. Andrea japo alikuwa wa kwanza kutajwa, na mtume wa kwanza kujiunga na Yesu, yaonekana hakuwa muongeaji sana, na mara nyingi anatajwa kama kaka wa Simoni Petro, japo ni yeye alimwita Petro. Kila mtu ana karama zake katika ufalme au shamba la BWANA; na karama ya Andrea ilikuwa kuwapeleka watu kwa YESU. Je umejiuliza karama zako ni zipi? Kuna maswali ambayo unaweza kuyapata ambayo yanakuonyesha karama yako unapoendelea kuyajibu! Je! Ni watu wangapi waliofunga kwa siku 40 kwenye Biblia?

Yesu alichagua wanafunzi hawa wavuvi, waliokuwa watu wa kawaida sana katika jamii ile, lakini watu hao walipokaa miguu pa Yesu hawakuwa tena watu wa kawaida. Kukaa na Yesu ni maarifa kupita yote, maana kuliwabadilisha watu hawa wa kawaida. Kiburi cha kisomo, kuwa na uwezo au mamlaka kimefanya wengi kumwacha Mungu au kunyanyasa wanyonge. Mitume waliingia kwenye kazi yenye changamoto nyingi, na mara nyingi walijiuliza kama kweli huyu wanayemfuata ndiye Mungu. Walijiuliza kwa nini wanapata shida na kuishi maisha ya chini kiasi kile. Wakaona hata aliyewaita Mwenyewe hana pa kuishi. Lakini baadaye walipoelewa hawakuendelea kujiuliza. Hata Yesu alipofufuka, hawakurudi chuoni, seminari, au kufanya biashara, bali waliendelea na kazi ya utume Yesu aliyowaachia.

Elimu ni jambo zuri "Mshike sana elimu. Ila Mungu anajua mara chache sana shule ya dunia inaweza kusaidia watu kuwa na hekima ya kufikilia wokovu au kumtii Yeye. Elimu kubwa imezungukwa na viburi, na kufanya wengi watumie talanta zao kwa kiburi na kuona wamejitosheleza. Hivi leo ukiwa shule kumbuka shule ya kwanza ni kujua Maandiko na kuyatii. Hiyo ndiyo shule ya dunia ya msingi, sekondari hata chuo.
Hiki ndicho Yesu alikuja kukifanya yaani kufa kwa ajili ya dhambi zetu, kuanzia dhambi za Adamu hadi za binadamu wa mwisho atakayeishi ulimwenguni. Yesu anachukua dhambi zetu, ulimwengu mzima, za kila mvulana au msichana anayemwamini. Na zaidi ya hilo, anavunja nguvu za dhambi kwa kutupatia nguvu ili tusitende dhambi. Kuna siku hivi karibuni, dhambi haitainua pembe zake milele zote. Yesu hakuwa na hofu, kuacha enzi, au kuendelea na mpango wa wokovu. Katika kila hatua aliamua kusonga mbele, mpaka siku ile aliyotundikwa msalabani. Hakushuka kwenye ule mti, ili wewe na mimi tuokolewe.

Hata leo wengi wamemua kujitoa kuwa wanafunzi wa Yesu, ili wapeleke ujumbe kwa wengine. Wameacha kazi nzuri, ndugu na jamaa na kwenda mbali kuhubiri. Wengine wameteswa shuleni, na kupata hasara kwa kumfuata Yesu. Yesu anaendelea kuita hata leo. Anahitaji wavulana na wasichana watakaokuwa wavuvi wa watu.
*MUNGU husikia maombi ya wote wanaomtafuta katika Kweli. Ana nguvu ambayo sisi sote tunahitaji. Anajaza moyo kwa upendo, na furaha, na amani, na utakatifu

---

Maswali: Kwa nini Yesu hakuwa na haja ya kumhakikishia Shetani kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu? Yesu aliwaambia wanafunzi Wake kwamba Yesu ni nani? Ni nani anachukua dhambi za uliwemwengu? Wanafunzi walipouliza "Rabi unakaa wapi" waljibiwaje? Elezea kazi ya Yohana mbatizaji. Je, unajua hata leo Yesu anakuita uwe mwanafunzi Wake?

**SIKU YA 202**
**(Julai 20)**

# Kuita wanafunzi wa kwanza

**Johana 1**



Andrea mwanafunzi wa kwanza wa Yesu, aliendа kumwita ndugu yake Simoni Petro, baada ya kusikia kutoka kwa Yohana mwalimu wake kuhusu Yesu. Kwa shauku na furaha alimwambia Simoni "tumemwona Masihi." Masihi ni Mpakwa mafuta, kwa lugha ya Kiyahudi au Kiebrania; yaani mfalme. Kristo ni Masihi kwa Kiyunani. Andrea akampeleka Simoni Petro kwa Yesu. Hata nasi leo tuwalete ndugu zetu, marafiki zetu na hata wazazi wetu kwa Yesu.

Tusikae kimya na habari za furaha na mafanikio kama hizi. Yesu akamtazama Simoni na kusema "Wewe u Simoni, mwana wa Yohana; nawe utaitwa Kefa." Tafsiri yake ni Petro au jiwe." Wana ndugu hawa wawili, Andrea na Simoni walikuwa wavuvi, katika bahari ya Galilaya wakitumia jarife. Yesu alipowaambia wamfuate alisema atawafanya kuwa 'wavuvi wa watu'. Hawa walipomfuata Yesu waliwaona wana wa Zebedayo, walioitwa Yohana na Yakobo wakiwa kwenye mashua ya baba yao wakikarabati nyavu za kuvulia samaki, katika biashara yao wenyewe ya uvuvi. Yesu akawaita na wakamwacha baba yao na chombo cha kuvulia, wakamfuata. Je, upo tayari kumfuata Yesu leo?

Wanafunzi hawa walitofautiana kitabia sana, ila wote walitokana na watu wa kawaida. Hawakuwa wamesoma shahada za vyuoni, au kutoka katika koo fulani zenye uwezo. Yesu alichagua watu wa kawaida, walio tayari kujifunza miguuni Pake. Hata leo tunapaswa tuwe wanyenyekevu na kujifunza ili tuwe kama Mwalimu wetu Yesu. Tunapata funzo kwa mitume kwamba watu hawana haja ya kufanana au kuwa sare kwa kila kitu, au kukubaliana kwa yote ndiyo wafanye kazi pamoja. Historia imeonyesha kumkubali Yesu na Neno Lake, kumebadilisha maisha na mioyo ya watu kuliko kitu kingine duniani au mbinguni.

Naye Yesu Siku ya pili akataka kuondoka kwenda Galilaya akamwona Filipo, akamwambia nifuate. Filipo alikuwa mtu wa Bethsaida mji mmoja wa Andrea na Petro. Filipo akamwona Nathanieli, akamwambia "Tumemwona Yeye, aliyeandikwa na Musa katika torati na manabii, Yesu mwana wa Yusufu mtu wa Nazareti." Nathanieli kwa mshangao bila hila au unafiki akasema lile alilolijua yeye na wengine " hivi kweli, laweza neno jema kutoka Nazareti?" Hiyo itakupa maswali na majibu, kama Nazareti ilikuwa ya namna gani! Filipo akamwambia "njoo uone."
Yesu akaona Nathanieli akija kwake, ndipo akanena kuhusu Nathanieli akisema "Mwisraeli kweli! kweli! hamna hila ndani yake." Hii ni sifa nzuri ambayo tungetaka sisi sote tuwe nayo! Nathanieli akashtuka "umepataje kunitambua?" Ndipo Yesu akamwambia, kabla Filipo hajakuita, "nilikuona ukiwa chini ya mti wa matunda ya tini." Hapo ndiyo Nathanieli akajua anazungumza na nani na akakiri "Rabi, Wewe u Mwana wa Mungu, Ndiwe Mfalme wa Israeli!" Yesu akamwambia umeamini kwa sababu nimekwambia nilikuona chini ya mti kabla hujaja? Hiyo tu? Sasa utaona mambo makubwa kuliko hayo" akamtahadharisha!

Kisha Yesu akasema Amin, amini nawaambia "mtaziona mbingu zimefunguka na malaika wa Mungu wakikwea na kushuka juu ya Mwana wa Adamu." Tukio hili la tumaini la baraka tutaliona mawinguni karibuni, maana tuko ukingoni mwa historia. Baadaye aliwaita Mathayo aitwaye Levi aliyekuwa kwenye kibarua chake cha kutoza ushuru na wengine. Jumla akawa na wanafunzi kumi na wawili aliofuatana nao, ambao majina yao yalikuwa Andrea, Yohana, Simoni, Yakobo, Mathayo, Nathanieli, Filipo, Thomaso, Bartolomeo, Yakobo wa pili, Yuda msaliti na Simoni wa pili. Yaonekana Yuda alijileta mwenyewe kwa kuona pengine atapata umashuhuri akijihusisha na mtu huyu wa ajabu, ila haioneshi kama aliitwa. Wanafunzi hawa walijulikana kama mitume baadaye.

Wanafunzi walikuja kwa Yesu kujifunza. Kisha wakawa mitume, yaani walitumwa kufundisha wengine; ila daima waliendelea kujifunza. Watu hawa walitofautiana sana kitabia. Si lazima ufanane na mtu na kukubaliana kila kitu na watu wa kanisa ili mfanye kazi ya Mungu. Inafurahisha kujua kwamba ni Yeye aliyewaita Yakobo na Yohana, wana wa ngurumo. Je umewahi kufikiri kuitwa mwana wa ngurumo na Yesu mwenyewe, kulimaanisha nini? Biblia itatueleza tunapoendelea na masimulizi. Yesu aliwabadilisha majina yao wengine walipofika Kwake. Hata leo anataka tupate majina au tabia mpya.

Wanafunzi wa Yesu walikuwa watu wa aina zote. Alikuja kuchagua baadaye wanafunzi 70 na kuwatuma wawili wawili waende kuhubiri. Hawa 70 walirudi wamefurahi

sana. Kulikuwa na uzuri wa kwenda wawili wawili kwani walipeana faraja, na pale mwingine alipopungukiwa kwa lolote mwingine alimsaidia. Hata wale 120 waliopokea Roho Mtakatifu walikuwa wanafunzi Wake Yesu. Hawa walipokea Roho Mtakatifu wakati wa Pentekoste. Ila wengi walimshuhudia Yesu kwenye huduma Zake za kila siku kwamba amewatendea makuu, nao hawawezi kueleza maana ni mengi na ya ajabu!

Katika Ufunuo 12:11, twaelezwa kuwa walimshinda Shetani kwa damu ya Mwana-Kondoo na kwa ushuhuda wa maneno yao. Wale waliopon ywa magonjwa walielekezwa waende wakawambie watu wa kwao namna walivyoponywa. Mwanafunzi ni mtu anayemkubali Yesu na kujitoa Kwake kikamilifu, na mahusiano yake huendelea kukua siku kwa siku. Mwanafunzi ni yule anayetaka kufanana na mwalimu wake, na anayefuata nyayo za mwalimu wake, katika nyanja zote, yaani kiroho, kimwili, kiuchumi, na kijamii. Kwa msaada wa Roho wa Mungu, anamweka Yesu mbele katika maisha Yake ya kila siku, iwe nyumbani, sokoni, michezoni, shuleni, kibaruani au katika nyumba ya ibada. Zamani zile wanafunzi walikaa kwa mwalimu (rabi) na kujifunza, kisha nao walienda kufundisha wengine.

Mwongofu ni yule anayekubali mafundisho ya mtu, ila mwanafunzi ni yule anayekubali mafundisho, na kuwaambia wengine ili wawe wongofu na wanafunzi. Ilibidi wanafunzi wajikane nafsi, na kubeba misalaba yao wakiwa tayari kumfuata Yesu kwa hiari yao. Kuna tofauti kubwa kati ya mwanafunzi na mshiriki wa kanisa. Hata leo tunaitwa wote kuwa wanafunzi wa Yesu. Mtu akiitwa na Yesu ni lazima aache kila kitu na kumfuata.

Huwezi kuwa mwanafunzi na ukaendelea kubeba vitu vyako vyote na kuendelea na maisha yako ya zamani. Yesu alisisitiza ni lazima kubeba msalaba. Cortez wa Spain alipofika Mexico akiwa ameteka eneo kubwa la nchi, na akiwa na wapiganaji 500, aliamuru kuchoma meli zote zilizowaleta, akimaanisha kwa wale wanajeshi wake “Watoe maisha yao kikamilifu kuchukua nchi hii” maana hakukuwa na ajenda ya kurudi nyuma. Mwanafunzi au Mkristo, lazima awe na kauli mbinu ya “mbele daima, nyuma mwiko.”

Kuna wengine ambao wangekuwa wanafunzi wa Yesu na walimjia Yesu, ila hawakuwa tayari kuacha vyote. Mfano ni kijana tajiri, kijana aliyesema anaenda kumzika baba yake, yule aliyetaka aage ndugu, hata marafiki na Nikodemu. Ila wengine Nikodemu alirudi na kubadilisha mawazo na kuwa mawanafunzi wa Yesu. Wanafunzi wengine walikuwa wanawake, na Yesu aliwatembelea makwao, wengine walimfuata na kumhudumia. Hawa ni kama Mariamu, Susana, Martha, Yohana, na wengine waliokuwa na imani baada ya Yesu kuwaponya.

Wanafunzi wengine walikuwa si Wayahudi, kama mwenye ukoma aliyerudi kutoa shukurani, mwanamke Msamaria wa kisimani au Jemadari wa Kirumi. Wanafunzi wote, ilibidi wajikane nafsi zao na kujitwika msalaba wao, kisha wamfuate. Nasi hatuwezi kumfuata Yesu na kuendelea kufanya mapenzi au matakwa yetu. Imani yetu katika Masihi haituruhusu tufanye tutakavyo! Hatuwezi kuwa wababe au jeuri, uasi ni kitu cha kutisha, tunaweza kuwa wakaidi katika Kristo kama Paulo, ila si wakaidi katika nyama na damu au miili yetu. Hivyo ni lazima tukae ndani

Yake, tujisalimishe Kwake na Kujazwa na Roho Wake Mungu. Mawazo na nia zetu ziongozwe na Roho wa Mungu. Kisha matendo yetu yatakuwa matunda tu ya mawazo, nia au shauku zetu.

Yesu akazunguka kote Galilaya akiwa na wanafunzi wake, akifundisha katika masinangogi, akihubiri habari njema ya ufalme, na kuponya magonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu. Kutokana na huduma yake ya uponyaji, vipo vijiji ambavyo vilikosa wagonjwa kabisa kwa kuwa wote walikuwa wameponywa. Alijua mtu ataweza kusikiliza habari njema za Mungu, ikiwa hana maumivu. Wakakumbuka nabii Isaya alivyosema "aliutwaa udhaifu wetu na kuchukua magonjwa yetu." Habari Zake zikaenea Shamu yote, na watu wakamletea wagonjwa, wenye maradhi mbali mbali kama walioteswa na pepo, wenye kifafa, walipooza, waliozimia, hata waliokufa, Naye akawaponya.

Makutano mengi wakamfuata kutoka miji ya Galilaya, Dekapolisi, Yerusalemu, Uyahudi, na hata ng'ambo ya mto Yordani. Kwenye zahanati wateja wakapungua huenda baadhi ya zahanati ilibidi zifungwe. Zamani matabibu walikula kiapo cha huduma kwa watu bila hila, ila vyama vya matabibu vya magharibi, mara zingine, vimefanya mipango fulani, ili matabibu wanufaike. Bali wakati wa Yesu, watu waliotibiwa hawakuhitaji kulipia matibabu, kulazwa, kuuguza vidonda, bimaa au kupewa dawa za maumivu baada ya upasuaji. Ila bado walimwua, japo aliwapa faida tu, hii inaonyesha kwamba moyo wa binadamu una magonjwa ya kufisha, na hakuna anayeujua njama zake mbaya isipokuwa Mungu! Kila mtu ameweza kujishangaa mwenyewe kwanini alifanya uovu fulani, hii inatuonyesha hatuko salama tunapojitegemea wenyewe, Biblia inaonyesha kwamba msichana mtanashati kabisa anaweza kumwua mtoto wake au kula uzao wa tumbo lake wakati wa njaa au taabu fulani kama hamweki Mungu kuwa kipaumbele!

Yesu alikuja kuwapa watu uzima wa milele. Ingawa wale waliofufuliwa au kuponywa walikufa baadaye, pengine baada ya miaka 50 au 60 hivi lakini ukweli ni kuwa Yesu alikuwa amewatambulisha kupokea uzima wa milele, ili waishi bila kikomo. Uzima wa milele haihusu muda fulani tu cha kuishi, bali ni kumjua Yesu. Yesu anatuambia "Na uzima wa milele ndiyo huu, wakujue Wewe Mwenyezi Mungu wa pekee, na Yesu Kristo uliyemtuma." Kule kumjua tu, ndiyo uzima wa milele, mbali na kule kuishi muda mrefu.

Watu walishangaa jinsi alivyojua kila kitu wakati hakuwa ameenda chuo kikuu au hata sekondari ya marabi. Kilichowavutia zaidi ni jinsi alivyojali kila mtu, bila kujali ni mvulana, msichana, mtoto, mwanamume, tajiri, mrefu, mfupi, mnene, mweusi, maji ya kunde, mweupe, mama, au baba. Yesu alijua Neno la kusema kwa kila mtu; maneno ya upole, ya kutia moyo, na kumfanya mtu ajisikie vizuri. Baada ya mtu kuwa naye kwa dakika chache tu, aliendà na moyo wake ukiwa na furaha na joto.
Biblia inasema watu walishangazwa juu ya mafundisho Yake. Yeye Ndiye tunu yetu kubwa, binadamu wote. Tukiwa Naye, daima mioyo yetu hufurahi na kuburudika, na ndiyo maana mbinguni itakuwa mahali pa ajabu, furaha na amani, kwa vile atakuwa nasi, milele na milele. Tumegundua kwamba mbinguni, si vile vitu na utajiri uliopo, japo navyo ni vizuri kwa kuviangalia, kuvionja, au kuvihisi, bali ni kule kuwa

na Yesu na mioyo yetu kuburudika, na kuwa na furaha isiyo na kikomo. Biblia yasema, Onjeni na kuona wenyewe jinsi Mungu alivyo mwema.

Ni tunu iliyoje wanaume hawa 12 walikuwa nayo, ya kualikwa na Yesu Mwenyewe kuwa wanafunzi Wake. Majina yao yameandikwa kwenye misingi ya mji wa Yerusalemu mpya. Hata wewe una nafasi hiyo leo ya kuwa mwanafunzi Wake. Je uko tayari kuwa mwanafunzi Wake unapoishi?

*MUNGU husikia Maombi kwa ajili ya kuongoa Roho — Wakati wale wanaojua Ukweli wanapofanya mazoezi ya kujikana nafsi yaliyoamriwa katika Neno la MUNGU, ujumbe utaenda kwa nguvu. Bwana atasikia maombi yetu ya kuongoka kwa roho. Watu wa MUNGU wataacha nuru yao iangaze, na wale wasioamini, wakiona matendo yao mema, watamtukuza Baba yetu wa mbinguni.

*Tunapaswa kuja kwa MUNGU kwa imani, na kumimina dua zetu mbele Yake, tukiamini kwamba atafanya kazi kwa niaba yetu, na kwa niaba ya wale ambao tunatafuta kuwaokoa. Tunapaswa kutumia wakati mwingi kusali kwa bidii .
----------------------------------

Maswali: Nani alikuwa mwanafunzi wa kwanza wa Yesu? Wengine ni nani waliokuwa wanafunzi kwa kwanza wa Yesu? Nathanieli alisema nini, Yesu alipozungumza naye? Yesu alienda miji gani kuhubiri? Yesu alichagua wanafunzi wangapi? Kinyume cha uzima wa Milele ni nini? Je wewe ni mwongofu au mfuasi wa Yesu?

**SIKU YA 203**
**(Julai 21)**

# Yesu anafanya muujiza wa kwanza kwenye arusi Kana.

**Yohana 2.**



Baada ya kuita wanafunzi, Yesu alienda kuhudhuria harusi, kwao Kana ya Galilaya kama mtu wa kawaida, jirani, rafiki au ndugu. Alianza huduma Yake kwa kujichanganya na watu katika furaha yao. Alitaka kuvunja kuta zilizowatenganisha watu katika jamii ili wajue kuwa wanadamu wote tu familia moja ya Mungu. Ilikuwa imepita miaka 400 bila nabii, na sasa watu wanamwona Yohana Mbatizaji na kisha Yesu, ambao wanabadilisha maisha yao. Watu hawa wawili, walionekana wakiishi maisha rahisi na ya umaskini wa mali.

Hata katika jumuiya yetu ya leo inayojali mali, ufahari na kujionyesha, ule mfano wa Yesu wa kuwa masikini, na mnyenyekevu, ni mfano wa kuigwa unaohitajika kwetu sote. Kama Yesu angekuja kama Mfalme, angetufundisha kwa namna gani unyenyekevu na kuhudumia watu kwa huruma na upendo? Isitoshe, kama Yesu angekuja kama Mungu, ni binadamu gani, angeweza kustahimili ule utukufu na

fahari ya mbingu bila kuteketea? Kweli hubiri letu la kwanza si yale tunayosema, bali vile tunavyoonekana na kutenda.

Ilikuwa desturi ya Yesu kuwatambulisha wanafunzi wake kwa marafiki mbalimbali, alikwenda pamoja nao katika sehemu tofauti-tofauti ikiwepo na harusi ya Kana. Siku zile watu walisherekea arusi kwa pamoja na jirani zao, kwa siku kadhaa. Vijana wa umri Wake walianza kusikia kwamba amekuwa mhubiri wa ajabu. Wakaanza kuzungumza kwamba Yohana mbatizaji alimtaja kuwa ni "Masihi." Mazungumzo yaliendelea wakati watu wakifurahia arusi. Katika harusi ile, watoto kwa vijana hawakutengwa kama tufanyavyo leo, bali walikuwa na nafasi katika hafla hiyo. Ni makosa kutowaalika watoto kwenye arusi, maana ni tukio takatifu wanalopaswa kujifunza! Huenda mambo ya kadi za mwaliko hayakuwepo siku hizo. Watoto wasitengwe kwenye harusi, hili ni jambo baya. Kisingizio cha kuwalinda 'watu wazima wafanye mambo yao ya faragha yasiyofaa kuonwa na watoto' kama vile kunywa pombe au madai ya kubana matumizi ya chakula hakina mashiko kwa Mwenyezi Mungu.

Basi maji ya zabibu au divai ilipokwisha mama Yake aliingiwa na hofu, na kuhofia ile furaha waliyoanza nayo ingebadilika na kuingia doa karamu yao. Mama alimsogelea Yesu na kumwambia "Hawana divai." Hata leo ukiwa na sherehe hutapenda chakula au kinywaji kiishie katikati, bali ungependa uchafue meza na watu wasimulie hapo baadaye kuwa, "arusi ile ilifana sana." ila fanya mambo kwa kiasi, ukiweka akiba ya kuanzia maisha! Mama alijua mwanawe ana uwezo wa namna fulani kuwasaidia kukidhi hitaji hili. Yesu alijibu "mama, nina nini mimi nawe? Saa Yangu haijawadia kutokana na mipango ya mbingu." Yesu alimpenda mama Yake, ila alipenda kumtii Mungu kwanza. Mama Yake alikuwa ana imani na akaenda kuwaambia watumishi "Lolote atakalowaambia fanyeni." Wafanyakazi wakatii maagizo hayo.

Basi kulikuwa na mabalasi au mitungi mikubwa sita ya mawe, Yaliyokuwa yanawekewa maji; kila moja lilikuwa na lita 100 hivi, jumla lita 600. Yesu akawaambia wajaze maji, nao waliyajaza hayo mabalasi sita mpaka juu. Kisha akawaambia wachote na kumpelekea mkuu wa meza, au mshereheshaji (Master of Ceremony MC). Lazima wale watu walijiuliza kama waliyoelekezwa na Yesu yangekuwa msaada kweli katika kupata kinywaji kipya? Ila maji yalipogeuzwa kuwa kinywaji kizuri, mkuu wa meza yaani yule ashugulikiaye na sherehe alipoonja, bila ya kujua kilipotoka kinywaji hiki, akasema "watu huandaa divai njema na wakiisha kunywa sana ndiyo huleta ile dhaifu iliyotiwa maji mengi, ila wewe umeiweka divai iliyo njema ukaitoa mwishoni."

Unadhani ni zawadi gani bora waliyopata maarusi hawa zaidi ya hii? Walikuwa na bahati kwamba BWANA Mweyewe amehudhuria harusi yao, na kisha amewapa zawadi ya kinywaji. Yesu Ndiye atoaye vilivyo bora zaidi ya vilivyotangulia, na kuleta furaha na amani mioyoni mwetu. Kwa Yesu, sisi wanadamu au kanisa la Kikristo, ni bibi arusi Wake, na anataka tuwe na furaha. Anatufurahia leo kama bibi harusi Wake, akiwa na lengo la wote watakaomkubali atupeleke nyumbani kwa Babaye, kuishi Naye milele zote.

Kwa vile 40% ya watu ambao huanza kunywa kileo huishia kuwa walevi wa kutupwa, na kwa vile walevi hawaingii mbinguni kutokana na maelezo ya kitabu cha Ufunuo, hatuamini kwamba Yesu alibadili maji yale mengi kuwa kileo, bali aliyafanya maji yale kuwa kinywaji kizuri cha mizabibu. Biblia inasema "Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima." Asilimia 50 ya ajali zote barabarani zahusiana na kulewa. Magomvi ya nyumbani na uovu mwingi, kama wasemavyo watu, hutokana na unywaji wa pombe. Wengi wamesema pombe ni pepo au Shetani. Hekima ya mbingu inaelekeza usitumie hata tone moja la pombe kama anasa.

Mvinyo kwa lugha iliyotumika katika kisa hiki, ulikuwa na maana mbili, uliochachuka na kuwa kileo, au juisi ya tunda la mzabibu isiyochachuka. Mvinyo pia huwakilisha damu Yake iliyotuokoa na dhambi zetu. Yesu mwenyewe ni mnadhiri, hivyo itakuwa shida kubwa kama damu Yake itakuwa na kileo cha kuharibu maisha ya watu.
Huu ndiyo muujiza wa kwanza alioufanya Yesu, akaudhihirisha utukufu Wake, na wanafunzi Wake wakamwamini na mashaka yao yakapungua kidogo. Watu wakasimuliana jambo hili tena na tena.

*Kumbuka kwamba kufaulu kwa karipio kunategemea kwa ukubwa roho ambayo kupitia kwayo onyo linatolewa. Usipuuze maombi ya dhati ili uwe na roho ya kujishusha, inayonyenyekea, na kwamba malaika wa MUNGU waende mbele yako na kufanya kazi juu ya mioyo unayojaribu kuifikia, na hivyo wailainishe kwa hisia za mbinguni ili juhudi zako zipate kuwa zenye faida.
----------------------------

Maswali: Muujiza maana Yake ni nini? Kunywa Pombe ni dhambi, unaweza kuelezea mafungu ya Biblia? Sherehe ya arusi inapasa iweje?

**SIKU YA 204.**
**(Julai 22)**

# Yesu apindua meza za hekalu, na kutakasa hekalu.

**Yohana 2.**



Yesu alifanya muujiza wa kwanza kwenye harusi akionyesha kwamba ndoa ni ya muhimu, na kuthibitisha kuwa kufunga ndoa ni jambo la kipaumbele. Ndoa bora ni ile yenye pembe tatu, Mungu kwanza, ndipo mume na mke. Mtu asikae na mwanamke au mwanamume bila kufunga ndoa. Ndoa inayotambulika ni ile inayofungwa kwenye nyumba ya ibada, serikalini au ya jadi. Jambo jingine tunalojifunza ni kuwa ili sherehe iwe nzuri ni lazima iwe na adabu. Watoto wengi siku hizi, hawaalikwi harusini kwa makosa, kwani watu wameingiza uovu mwingi kwenye harusi na wanaona aibu kufanya vitu hivi mchana, ndipo wanavifanya usiku wa manane. Sherehe za usiku wa manane pia zinachosha watoto maana hupata usingizi.

Tunapofanya harusi tutilie makini yale tunayofanya wakati wa sherehe. Lazima tuwe Wakristo wakati wa sherehe pia, kama tulivyokuwa wakati wa ibada ya ndoa. Tujiulize, "Je hapa nilipo kama Yesu angekuja angefurahi au angehuzunika kuona tumepachagua kufanyia huduma hii nyeti?" Je nguo tunazovaa, maneno tunayosema, vyakula tunavyokula, na matendo yetu vina usafi ndani yake? Wale wakuu wa karamu wawe makini kwa kutosema vitu ambavyo havina utukufu kwa Mungu eti bora viwe vinachekesha au ni vya futuhi! Hebu wasiwe watu wanaoitwa "msema chochote" (MC); bali mwuungwana anayesema maneno yanayobariki watu. Tunaishi wakati ambao inatubidi tuwe waangalifu, katika matumizi yetu ya fedha kwa kuepuka kufanya sherehe ambazo mali huharibiwa; mali ambayo ingesaidia watu wenye mahitaji kama ada ya shule, chakula, nguo, nyumba bora au injili.

Harusi ilipomalizika, Yesu akatoka Kana ya Galilaya na kuelekea kule Kapernaumu akiwa na mamaye na nduguze. Huu ndiyo mji ambao Yesu alifanya miujiza yake mingi. Wanafunzi Wake wa kwanza wale wakina Andrea walitoka hapa, na ndiyo waliomwalika kwao. Yesu anafurahi tukimkaribisha. Aliutembelea mji huu tena na tena, akifanya miujiza mingi hapa. Kisha akashuka kwa siku kuu ya Pasaka hekaluni Yerusalemu na akaona watu wakiuza ngombe, kondoo na njiwa wa dhabihu.

Kelele za wanyama hawa na za watu zilifanya hekalu liwe mahali pa fujo na kelele. Wengine walikuwa wanabadilisha pesa ili wapate shekeli ya hekalu iliyoitwa Drakma ili watoe kodi. Mazungumzo ya kunadi au kupunguza bei, yalifanya hata watu wasisikie kinachoendelea ibadani. Kulikuwa kama kuna aina ya ulanguzi kwenye kupata hii shekeli ya hekalu. Makuhani walijua kuna kasoro, ila hawakujali hilo. Walikula rushwa kutoka kwa wafanya biashara, wakawa na ubia kuendeleza uharamia au wizi huu. Watu waliotoka mbali bila kafara, ilibidi wanunue hapa na bei ilikuwa ya ulanguzi.

Yesu alifanya kifimbo cha kamba au mkoto na kuwatoa watu wote pamoja na wanyama hekaluni. Alimwaga fedha za wenye kubadili fedha na kuzipindua meza zao; akawaambia "Yaondoeni haya, msifanye nyumba ya Baba Yangu kuwa nyumba ya biashara." Akawaambia nyumba Yake itaitwa nyumba ya sala na siyo pango la wanyang'anyi. Watu walikimbia walipotazama uso Wake na kuona utukufu, na wala hawakujaribu kujadili Naye au kubishana. Makuhani walikuwa wamepoteza mahusiano na Mungu kiasi cha kusahau kafara hii ilikuwa inamwakilisha Masihi, Yesu ajaye. Hata leo hatuwezi kutoa uovu mioyoni mwetu, bali ni Yesu tu, Ndiye awezaye kutusaidia kufanya hivyo. Lakini wafanya biashara na makuhani hawakupenda kupoteza mamlaka na pesa kutoka kwa watu, hivyo walizidi kuchukia kitendo kile cha Yesu.

Wanafunzi Wake wakakukumbuka unabii usemao "wivu wa nyumba Yako utanila." Wayahudi wakamwambia awape ishara kwa nini afanya hayo. Akawajibu "vunja hekalu hili, Nami katika siku tatu nitalisimamisha." Wayahudi wakashanga kwamba lile hekalu lilichukua miaka 46 kujengwa na bado lina mapungufu, Yeye atawezaje basi kwa siku tatu kulibomoa na kulijenga. Walishindwa kumuelewa Yesu kuwa alikuwa akizungumzia kuhusu mwili Wake. Wanafunzi walikuja kuelewa alipofufuka baada ya siku tatu. Hata hivyo hilo la kujenga hekalu kwa siku tatu BWANA anaweza kulifanya hata kwa sekunde moja. Lakini Yesu alitaka kutufundisha tuepuke kufanya nyumba ya Mungu kama sehemu ya kujipatia faida au kujiburudisha.

Je Tunanong'onozena tukiwa kanisani? Je, tunacheza, au kuangalia simu au Ipad zetu tukiwa kanisani kwa namna inayotutoa ibadani? Je tunajipitish-pitisha na kutembea tembea wakati ibada inaendelea? Je tunajua maana ya kuja ibadani au tunakuja kwa mazoea tu kwa vile wazazi wanatuleta na kuanzia mababu zetu watu walikuwa wanakwenda ibadani? Ibilisi aweza kuwasindikiza watu ibadani, ikiwa hawako tayari kumwabudu Mungu bali kufanya mapenzi yao. Nyumba ya Mungu ni nyumba ya sala, si mahali pa biashara au shughuli zetu. Kilikuwa kituko cha ajabu watu kutoka hekaluni wakikimbia katika mji huu mkuu wa Yerusalemu. Habari hizo zikaenea kila mahali, wakakumbuka maneno ya Yohana mbatizaji "Tazama Mwana-Kondoo wa

Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu."

Watu wengi wakamwamini Yesu katika siku kuu hii, kwa ishara alizofanya. Ila Yesu hakuweka matumaini Yake kwa watu hawa; kwa kuwa alijua yote yaliyo ndani ya mioyo ya wanadamu, kwamba hubadilika badilika na pengine hata huwa feki (unafiki). Hakuhitaji mtu amwambie wanachofikiri, kwa vile alijua kila wazo lao. Wao walimkebehi walipomwendea, wakitaka kumjaribu ili waone 'atasema nini', wasijue Yeye aliwaona huko waliko kabla hawajafika Kwake, na kusoma mawazo yao yote. Ila alikuwa si kama mimi, ambaye ningewaambia 'wanajisumbua' na kuwaambia kwamba mawazo yao ninaysoma kama mionzi ya Xray. Yeye alitafuta njia ya kuwasaidia waokolewe. Shida zilizojulikana siku zile za mafarisayo, waandishi, makuhani na wazee, ni kiburi, unafiki, upofu wa kiroho, kutokuwa na rehema, na uovu. Shida hizi tunazo hata leo, hebu tumwombe Mungu atubadilishe. Ni vyema tukae katikati kwenye injili, kushoto ni unafiki, kulia ni udunia, tukae katikati kwenye msalaba, ndiyo kuwa ndani Yake Masihi. Tumwombe atusaidie!

Yesu hakufanya muujiza kwenye baraza la viongozi wa dini yaani Sanhedrini kule Yerusalemu, bali kwenye kijiji duni, ili kuongeza furaha, kwa watoto na watu wazima wa kijiji kile. Alionyesha shauku na nia Yake ya kutaka kuwapa furaha.
*Ikiwa watu kadhaa wangekutana pamoja kwa nia moja, na mioyo iliyolemewa na mzigo kwa ajili ya roho zinazoangamia, na watoe maombi ya dhati, ya bidii, hakika matokeo yangekua mazuri.

----------------------------

Maswali: "Lolote atalowaambia fanyeni", hii sentesi inatuhusuje leo? Mkuu wa meza alisema nini kuhusu divai? Unafikiri ni Kwa nini Yesu alifanya muujiza wa kwanza kwenye harusi? Kwa nini watoto waalikwe harusini? Kwa nini mtangazaji kwenye sherehe (MC) awe mwangalifu wa maneno yake kwa kukuwa msema chochote cha upuuzi? Kwa nini kufunga ndoa ni muhimu? Taasisi ya Ndoa ilitoka wapi? Jadili jinsi ya kuenenda kanisani, kwa kutumia kitabu cha Shuhuda, gombo la Tano, sura ya 55! Kama hauna tuandikie tukutumie, asante!

**SIKU YA 205.**
**(Julai 23)**

# Nikodemu mwanafunzi wa Yesu aliyekuja usiku.

**Yohana 3**



Baada ya kupindua meza na watu kutimua mbio, baadaye watu walirudi na kuendelea na kazi zao bila kujali. Walipewa kutafakari na kuacha makelele nyumbani mwa BWANA. Wengine walijishangaa-shangaa kwa ule woga uliowaingia hadi wakakimbia. Wengine walikasirika kwa kuwa watu waliwacheka kwa kukimbia, na wengine wakawa na visasi Kwake Yesu mioyoni mwao. Makuhani hawakupenda jambo hili, maana walikuwa wanapata faida za namna fulani za kibinafsi. Nao wakaona mapato na hadhi zao vimeshushwa chini. Hekalu lilikuwa linaingiza mamilioni ya pesa kuliko biashara nyingine yoyote. Uchumi wa Israeli wote ulijikita kwenye utoaji wa kafara. Wanyama wa kafara walikuwa Ghali, jambo lililosababisha makelele mengi ya wale wanaonadi wanyama hao. Jambo hili lilipoteza utukufu wa kafara ya Mwana-Kondoo wa Mungu aliyekuja kuwa kafara halisi.

Hekalu kwao lilikuwa mahali pa kuchumia mali, na si pa kutafakari wokovu. Hata hivyo, kulikuwa na watu walikuwa wameanza kumwamini, au kutafakari kazi zake.

Mmojawapo wa watu hao ni kiongozi wa mafarisayo, jina lake Nikodemu, kiongozi wa baraza la wazee wa Kiyahudi la Sanhedrin. Wakati Israeli ilipokuwa huru, lilikuwa baraza la mwisho au korti kuu ya nchi. Baraza hili, lilitunga sheria za dini na za nchi na kuhakikishwa zinatunzwa au kudhibitiwa; ila Wayahudi walipotawaliwa na Warumi, na sheria zao, nguvu zake zilipungua kiasi fulani.

Walihitaji uamuzi wa mwisho wa mamlaka ya Rumi kumhukumu mtu kwa mambo fulani. Wajumbe wa Sanhedrin walikuwa wamechaguliwa kutoka kwa makuhani, walimu na viongozi. Kuhani mkuu kwa kawaida alikuwa kiongozi mkuu wa hawa watu 71. Mafarisayo walikadiriwa kuwa kama 6,000 hivi; hawa walijulikana kama vinara wa mambo ya kidini. Wengine waliohusika na mambo ya uongozi wa dini walikuwa Waandishi na Makuhani.

Nikodemu, Alisikia habari Zake Yesu hekaluni, akataka amjue zaidi. Huyu alimjia Yesu usiku, akiogopa watu wasimwone. Baada ya kupeleleza peleleza anapopatikana, alipata habari kwamba Yesu huenda, mahali gani, usiku kupumzika na kuomba. Tukumbuke kwamba ni bora kwenda usiku ukijificha kwa Yesu, kuliko kutokwenda kabisa! Huyu alikuwa shujaa, kiasi fulani ukilinganisha na mafarisayo wenzake. Basi alimtafuta Yesu na alipofika pale, akaanza kumsifia "Rabi, twajua kuwa u mwalimu na umetoka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo Wewe." Rabi huyu alitafuta mahali pa kuanzia mazungumzo akitaka angie katika mjadala wa kina na Yesu. Ila Yesu ajuaye mioyo ya watu, hakuhitaji mtu amwambie kuhusu watu, maana aliwajua nje na ndani.

Tukitaka kuwa Wakristo hatuhitaji kujadili na kubishana, bali kubadilishwa mawazo na nia zetu, ili tuwe na upendo wa Kweli wa Yesu. Yesu akamweleza miujiza pekee si tosha kuamini ufalme wa Mungu ila "Amini Amini nakuambia mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuona ufalme wa Mungu." Nikodemu hakuhitaji kuwa na elimu kubwa ili kuelewa jibu la maswali yake, bali moyo uliozaliwa upya kupitia Roho Mtakatifu. Hatuwezi kuelewa ufalme wa mbinguni, ikiwa hatuna maisha haya mapya toka juu mbinguni. Nikodemu akashangaa mtu awezaje kuzaliwa mara ya pili akiwa mzee "awezaje kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?" Yesu akajibu "Amini amini nakuambia mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu."

Yesu akasema upepo huvuma lakini hatuuoni kwa macho lakini tunajua kuwa upo kutokana na matokeo yake. Hata mtu aliyezaliwa mara ya pili, haoni Roho itendavyo kazi ila anasikia na kuona zile kazi zake njema au matunda yake. Wengi hata leo hufikiri kwamba Mungu ni Baba wa watu wote, na kwa hiyo hakuna umuhimu wa kujishikamanisha na ushirika fulani. Ni kweli Mungu ni Baba wa wote, bali kuzaliwa kwa Roho na maji ni kuwa Mwana Wake kwa aina ya pekee, na kuanza maisha mapya. Hatua hii humlazimisha aliyezaliwa mara ya pili kujiunga na kundi la waumini alioamini kwao, ambao wanafuata amri za Mungu na maagizo Yake, ambayo ni Biblia, ili akuzwe kiroho. Ni vigumu kuwa nyuki bila mzinga na watu watajua sisi ni wakristo kwa upendo wetu ndani ya ushirika, watauonaje upendo huu kama hatukutani basi? Wengi wameumizwa kwenye ushirika fulani, basi tumwombe Mungu atupe kupona, na pengine tuhame pale mahitaji yetu yanaweza kukidhiwa.

Nimefanya hivi mara moja katika maisha yangu. Kwa upande mwingine upo Ukweli kwamba wapo wanaozaliwa kwa maji kwa njia ya ubatizo na kuwa washiriki wa kanisa mahalia, ila wanakuwa hawajamkubali Yesu kuwa Mwokozi wao mioyoni, yaani hawajaacha maisha ya zamani na kuzaliwa kiroho, au kumpokea Roho wa Mungu. Hayo ni makosa pia.

Nikodemu akashangaa, kwamba haya yawezekanaje? Yesu akamwambia "Je wewe u mwalimu wa Israeli mambo haya huyafahamu." Yesu, akamwambia akisema, mara nyingi watu hawasadiki, na itakuwa vigumu kusema hata vile vya mbinguni kama vya duniani wanavyoviona, hawasadiki. Naye akasema kuhusu wokovu anaowapa watu wanaomtazama na kumtumaini akimkumbushia yaliyotokea jangwani "kama vile Musa alivyomwinua Nyoka jangwani, vivyo hivyo Yeye Yesu hana budi kuinuliwa ili kila mtu amwaminiaye awe na uzima wa milele. Kisha akamwambia Maneno makuu na mazito, kupita yote. Usomapo, waweza kuweka jina lako pale inaposema ulimwengu na kila mtu amwaminiaye.

Yesu akamwambia Nikodemu "Kwa maana jinsi hii, Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiaye asipotee, bali awe na uzima wa milele'. Basi sisi twaweza kusema hivi "Kwa maana jinsi hii, Mungu alimpenda Amina hata akamtoa Mwanawe pekee, ili Daudi, au Danieli, au Paulo, au Neema, akimwamini, asipotee, bali awe na uzima wa milele." Mungu hakupenda tu nchi ya Korea, au Somalia, au Brazili bali ulimwengu wote. Hii humaanisha wewe na mimi pia. Tukimwamini hapo hapo tunapata uzima wa milele, tukisubiri hali ya kutokufa ambayo Mungu atatuzawadia, atakapokuja mara ya pili.

Yesu hakuja kuhukumu ulimwengu ila kuokoa ulimwengu. Yeye anayemwamini hahukumiwi, bali asiyemwamini amekwisha kuhukumiwa. Kwani mtu asiyempenda Mungu hupenda giza, au matendo maovu. Tukipenda maovu twachukia nuru. Ila tukipenda nuru tunakuwa na ile Kweli na matendo ya nuru. Yesu hakuja ili watu waadhibiwe, La! hasha, bali ili tuponywe na kuokolewa. Ni rahisi mtu kumwokoa rafiki au mtu mwema, ila sisi Yesu alituokoa tukiwa wabaya bado, na wahitaji. Hakuna anayemwamini na kumtumaini Yesu atakayehukumiwa au ambaye matazamio yake yataangushwa. Ila mtu asiyemwamini, amejiadhibu mwenyewe kwa kukataa wokovu.

Yesu alitaka Nikodemu ajue kwamba Roho Mtakatifu anakuja wakati moyo wa mtu uko wazi kwake. Roho Huyu wa Mungu anabadilisha mawazo na hisia za mtu anayejikabidhi kwa Mungu. Hakuna anayejua jinsi Roho wa Mungu anavyoingia maana ni muujiza kwao wampendao Mungu; Ila matokeo yake yanaonekana wazi kama vile upepo usivyoonekana bali kazi zake zaonekana. Mvulana au msichana ambaye Roho wa Mungu anakuja kwake, huwa na upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole,kiasi, fadhili, na utu wema. Anapenda mema na kuchukia uovu.

Nikodemu alijua yote haya, ila kama farisayo alidhani yanawahusu wengine na si yeye. Alifikiri kwamba matendo yake mazuri yanayoonekana kwa nje yanatosha kumwokoa kabisa. Hivyo alikuja kufanya mjadala tu na mwalimu mwema, pengine akitaka kujionyesha kisomo chake cha hali ya juu. Ila akagundua ana mengi ya

kujifunza; ule wadhifa wake aliuona kama ndiyo wokovu, akagundua Mungu Ndiye anavika wanadamu vazi la haki na wokovu. Mambo aliyoambiwa Nikodemu yatuhusu nasi leo, japo yalizungumzwa kwenye giza la usiku miaka 2,000 iliyopita; yametangazwa kwenye radio, na wahubiri na magazeti dunia nzima, na ndiyo kitovu cha injili au habari njema. "Mungu anaupenda ulimwengu, Naye alimtuma Mwanawe, ili kila amwaminiye asipotee bali aupate uzima wa milele.". Hebu na tumwamini leo! Tunaposikia sauti Yake, tusiifanye mioyo yetu kuwa migumu, kwa Jina la Yesu Kristo, Amina! Ndilo ombi langu!

Nikodemu alimwamini Yesu kwa moyo wake wote, ila akili yake ilikuwa inampotosha, akitamani kuendelea kuwa na wenzake. Akaona ni vyema awe mwanafunzi au mfuasi wa Yesu kwa siri. Bado alikuwa anaona haya kuonekana na Yesu. Pengine alijiuliza akitoka usiku na kurudi kwake "Je ni kweli Yesu anaweza kuokoa wote wamjiao na kumwamini?" Hata leo hatuna haja kulipia wokovu wetu, Yesu anaweza kumwokoa kila mtu ajaye Kwake bure. Je unamwamini Yesu na kukubali kafara Yake? Ingiza kwenye moyo wako, upendo Wake, na kumwamini Naye atakuwezesha kupata unyenyekevu, na kutoa hasira, wivu au magomvi. Hii ndiyo maana ya kuzaliwa mara ya pili; Yesu anaingia, na anazaliwa mioyoni mwetu.

Nikodemu aliendelea kujificha ficha, japo alimtetea Yesu na mitume kwenye baraza lao la Sanhedrini. Yesu alipokufa, Nikodemu alijitokeza wazi wazi na kutoa manukato ya kupaka mwili wa Yesu na kuuzika pamoja na Yusufu wa Arimathayo. Kutokea pale twaamini, alitoka kwenye uvungu na kuwa shujaa wa Yesu. Hatuwezi kuwa uvunguni na kudai tunampenda Mwenyezi Mungu. Sisi ni taa, na watu wanapaswa waone nuru yetu ili tupate watakaoipokea, na kisha kuiambukiza nuru hiyo kwa watu wengine.

Yesu akaenda Uyahudi pamoja na wanafunzi wake, akiwafundisha huko. Wanafunzi wake walibatiza watu wengi, hata wanafunzi wa Yohana mbatizaji walianza kuona wivu kidogo kwa jinsi huduma ya Yesu ilivyokuwa inaenda kasi. Yohana furaha yake ilikuwa kubwa, kwa vile alikuja kuwafundisha watu habari za Yesu. Yohana, alikuwa akibatiza huko Amnoni, karibu na Salimu maana maji yalikuwa mengi huko. Huwezi kubatizwa kwa maji machache! Ubatizo, sharti mwili wote uwe ndani ya maji, ndiyo alama hii inakuwa imetimizwa kufuatana na Maandiko na Ubatizo wa Yesu Mweneywe. Wanafunzi wa Yesu na Yesu mwenyewe walikuwa wakiwabatiza watu kwenye maji mengi kwa kuwazamisha siyo kama vile ifanyikavyo leo mahali pengine. Huu ndiyo ubatizo ulivyoagizwa kufanywa kwenye Maandiko. Watu wakamwendea na kubatizwa, kabla Yohana hajawekwa gerezani.

Pakatokea mashindano kati ya wanafunzi wa Yohana na wa Yesu. Wanafunzi wa Yohana wakalalamika kuwa Yesu anabatiza watu wengi wanaomwendea. Yohana akawaambia mtu hawezi kupokea Neno la Mungu mpaka amepewa kutoka mbinguni. Akawaambia wanafunzi wake, kwamba ameshawaambia yeye si Kristo, ila ametumwa kumtangulia ili kutayarisha mioyo ya watu. Akasema yeye ni kama rafiki wa Bwana harusi, mambo yanapomnyookea bwana arusi, basi hiyo ni furaha yake kubwa. Yohana akasema furaha yake imetimia kwamba "Yeye Kristo hana budi kuzidi, na mimi kupungua."

Akasisitiza kwamba amwaminiaye Mwana wa Mungu ana uzima wa milele. Uzima wa milele unaanza kwa kumwamini, bali kutokufa tutavikwa Yesu akija mara ya pili. *Kuombea Nafsi Kutatuleta Karibu na MUNGU— Tunapotafuta kuwaleta wengine kwa Kristo, tukibeba mzigo wa roho za watu katika maombi yetu, mioyo yetu itadunda na ushawishi wenye nguvu wa kuhuishwa wa neema ya MUNGU; mapenzi yetu wenyewe yatang'aa kwa bidii zaidi ya kiungu; maisha yetu yote ya Kikristo yatakuwa halisia zaidi, yenye bidii zaidi, na ya maombi zaidi.

--------------------------

Maswali: Kwa nini ni uovu kupiga makelele kanisani? Nikodemu alikuwa nani? Yesu alimwambia apaswa kufanya nini ili kuingia mbinguni? Je unamwamini Yesu? Je umemkiri Yesu kwa midomo yako? Je umemkubali Yesu na kumwomba nguvu za kumtii? Kwa nini kulikuwa na mashindano, kati ya wanafunzi wa Yohana na wa Yesu? Yohana aliwajibuje wanafunzi wake? Yesu alibatizwaje kwenye Maandiko Matakatifu? Kwanini tunapaswa kubatizwa kama Yeye. Chukua muda kutafakari maana ya kuzaliwa mara ya pili!

**SIKU 206**
**(Julai 24)**

# Mwanamke Msamaria wa Sikari kisimani.

**Yohana 4**



Yesu akajua mafarisayo wamepata wivu kwa kusikia ana wanafunzi wengi zaidi ya Yohana mbatizaji, Naye akatoka Uyahudi na kwenda katika mji wa Samaria uitwao Sikari, karibu na shamba la Yakobo alilompa mwanawe, ambapo kulikuwa na kisima cha Yakobo. Wayahudi walijiona wao ni bora kuliko Wasamaria, japo zamani walikuwa jamaa moja. Waliona ni kusaliti kabila lao, kwa kuwa marafiki wa Wasamaria, wakajenga chuki nao nyingi kwa miaka zaidi ya 400. Yesu akiwa amechoka na mwenye kiu aliketi kisimani, kama saa sita mchana, na wanafunzi Wake walienda mjini wanunue chakula pengine kilichopikwa kutoka kwenye migahawa. Maneno haya yanatuonyesha Yesu alikuwa binadamu, anayesikia njaa, kiu hata kuchoka.

Akatokea mwanamke mmoja Msamaria ambaye Yesu alimkusudia apokee injili. Yesu alipanga ile safari akimfuata huyu mmoja tu, ili ampe Maneno ya wokovu. Yesu akamwomba maji ya kunywa. Mwanamke yule alishangaa akijua anayemwomba ni Myahudi kutokana na mavazi Yake. Akajiuliza inakuwaje Myahudi huyu kutaka maji kwa mwanamke Msamaria wakati wao ni maadui? Wasamaria na Wayahudi walikuwa wakikwepana kwa kadri walivyoweza. Japo jukumu la kumpa maji mtu, lilikuwa la muhimu hata kwa walio maadui, mama huyu bado alishangazwa na ombi la mtu huyu. Wasamaria walikuwa na vitabu vitano tu vya Musa, bila manabii wengine, walikuwa na mahekalu ila waliabudu tofauti na Wayahudi.

Kumbuka mji huu wa Samaria ulianzishwa na Ahabu na mke wake Yezebeli. Hawa walitoka kwenye ibada za kumwabudu Mungu wa kweli na kuharibu taifa zima. Mwanamke huyu Msamaria alimwona Yesu, ni kama Myahudi msafiri, mwenye vumbi na kiu kama wengine tu. Yesu alimjibu yule mwanamke "ungelijua karama ya Mungu, Naye ni nani akuambiaye nipe maji ninywe, ungelimwomba Yeye maji na angalikupa maji ya uhai." Mwanamke huyu akashangaa kwamba Yesu atapataje maji kwenye kisima hiki chenye kina cha futi 100, na hana cha kutekea hivyo akauliza

"umeyapata wapi maji hayo." Akamwuliza kama Yeye ni mkuu zaidi ya babu yao maarufu Yakobo aliyejenga kisima hicho?

Mama huyu alijua kwamba Yakobo ni baba wa imani na ilikuwa imepita zaidi ya miaka elfu wakitumia kisima kile, hivyo akajua Yakobo ndiye aliyekuwa mkubwa. Mama huyu ni lazima aliona uso wa Yesu wenye upendo, na huruma ndiyo maana hakukimbia, japo Yesu alikuwa mwanamume na Myahudi. Siku zile kuta za jinsia na za makabila zilitawala; mwanamke asingezungumza na mwanamume mahali pa wazi. Je sisi ni watu wa kujenga madaraja na watu wa makabila mengine au ni watu tunaopalilia tofauti zetu za makabila na jinsia na kuleta mafarakano?

Yesu akamwambia kila anywaye maji Yake, hataona kiu milele, bali yatakuwa chemichemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele. Wayahudi waliujua unabii huu wa Isaya 49:10 ambao ulimtambulisha Mungu kama chemchemi ya maji ya uzima. Shauku ya mwanamke huyu ikaongezeka, akamkodolea macho Yesu, akijua huyu si mtu wa kawaida. Roho wa Mungu alifanya kazi Yake, naye akamkubali kuongozwa na akawa tayari kuyaamini na kuyafuata Maandiko. Basi akayatamani hayo maji ili asije kila mara hapa kuteka na kutembea maili nyingi kurudi kwake kama jinsi tunavyojua kwetu Afrika shida ya maji ilivyo na matumizi yake mengi.

Akamwambia Yesu "BWANA unipe hayo maji, ili nisione kiu, wala nisije hapa kuteka maji." Yesu hakupoteza muda kujadiliana, au kubishana na mama Msamaria, bali alikazia ujumbe Wake wa wokovu, mwishowe, yule mama akavuviwa. Yesu akamwambia amwite mume wake, naye alisema hana mume. Yesu akamwambia amesema kweli kwani "umekuwa na waume watano, naye uliye naye sasa siye mume wako." Mama huyu akashtuka na kukiri "BWANA naona u nabii!" Mama huyu alikuwa anauliza maswali mengi, na kubadilisha mada au kichwa cha habari kila mara. Akasema baba zake waliabudu katika mlima huu, na watu wasema Wayahudi wanataka kuabudu Yerusalemu sasa wafuate lipi? Yesu alijua jinsi ya kumpa masomo rahisi ya Biblia (Bible Study).

Yesu akamwambia "saa inakuja watu hawatamwabudu Mungu katika mlima au Yerusalemu bali katika Roho na kweli." Akamwambia ni kweli Wayahudi wanajua wanachoabudu, ila kitakachojalisha ni kumweka Yesu mioyoni mwetu na si mahali. Moyo ni kiungo cha kusukuma damu, ila Biblia ikisema moyo ina maana nia, au ubongo. Yesu, akasema Baba Yake anatafuta wale ambao wako tayari kumwabudu, katika Roho na Kweli. Yule mwanamke alikuwa ameshajua Masihi atakuja na kwamba atakapokuja atawafunulia mambo yote. Yesu akamwambia bila mafumbo "Mimi ninayesema nawe Ndiye!"

Wanafunzi wa Yesu waliokuwa wamekwenda kununua chakula wakatokea, na kushangaa huyu mwanamke tena wa Kisamaria anayebadili-badili wanaume, akiongea na Yesu, ila wasimwulize bali wakamkaribisha chakula walichonunua. Yesu akawajibu anacho chakula wasichokijua. Wanafunzi wakaulizana kama kuna mtu alimletea chochote ale. Yesu akajibu "chakula Changu ni kutenda mapenzi ya Baba Yangu aliyenipeleka na kumaliza kazi Yake." Yesu alijua kwamba ni wakati wa kuvuna Roho ya huyu mwanamke wa Samaria na si wakati wa kula.

Hata leo tusipoteze nafasi kwa kujiingiza kwenye shughuli nyingi tunapokuwa kwenye kazi ya injili na wakati watu wako tayari kukata shauri kumchagua Mwenyezi Mungu. Akawaambia wanafunzi, wakati wa mavuno kila mtu anaujua na sasa umefika wakati wa kuvuna roho za watu. Akawaambia mavuno ni mengi bali watenda kazi au watu wa kuwaambia wengine ni wachache. Watu wengi hushughulika na mipango mbali mbali ya kufanya watu wakae kanisani nayo ni njema sana, yaani kushughulikia mazao yaliyo tayari ghalani. Ila Yesu alitilia sana mkazo kwa yale mavuno ambayo yako bado mashambani, yaani watu ambao hawajawahi kusikia habari za injili kabisa. Yote ni muhimu, Mungu atupe hekima Yesu akawaambia kila apandaye Neno la Mungu kwa watu au akusanyae atapokea mshahara. Yaani wenye kushughulikia mavuno yapatikane, wote watashangilia. Akasema wengine wanapanda kwa kuwafundisha watu, ila wengine wanavuna watu wanapofanya uamuzi kumfuata Mwenyezi Mungu wote hawa wanavuna mavuno ya uzima wa milele. Wanafunzi hawakuelewa ila walipoona wale Wasamaria na yule mama wanapiga mbio na kukubali injili ndipo wakaelewa mavuno yale ni yule mama na wale Wasamaria wakasema "Tumeona wenyewe, sasa twajua huyu Ndiye mkombozi wa dunia yote." Kumbe wanafunzi walikuwa wagumu kumwamini Yesu kuwa ni Masihi, hadi waliposhuhudia kwa macho yao jinsi watu wanavyomwamini. Mama huyu alijua dhambi yake, na hakuwa na kiburi au kujisikia ametosheka kama walivyokuwa wale mitume. Tukumbuke kila mfuasi wa Yesu ni mmishonari.

Basi yule mama Msamaria alipiga mbio kijijini kwake akasahau mtungi wake kisimani. Akaenda akawaita watu wa mjini kwake, akawatolea ushuhuda wake, na wengi wakamwamini Yesu siku ile. Aliwaambia watu "njooni mwone yule aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda." Mwanamke huyu Msamaria mara akawa mwanafunzi wa Yesu! Yesu alikuwa akitoa matumaini kwa wote, na hata kwa wale waliotengwa au kushindikana na jamii kama wenye magonjwa ya akili, vilema, wafungwa, wasio na makao, mashoga, watoza ushuru, wezi, wavuta bangi, walevi, waasherati, watu wanene kupita kiasi na wengine. Aliwapa matumaini wote kwamba wanaweza kuwa watoto wa Mungu wakichagua kumtii.

Twapata somo hapa kwa mwanamke huyu, kwamba inatubidi tujifunze kumwamini Mungu kikamilifu. Wakati wa Yesu hakuna binadamu ambaye alikuwa hana faida Kwake. Hata wewe waweza kuwasimulia watu matendo makuu ya Mungu aliyokutendea na kuwa mwanafunzi wa Yesu leo. Wengi siku ile, wakamsihi Yesu akae kwao, Naye akakaa siku mbili, wengi wakaamini kwa ushuhuda wa yule mwanamke kwamba Yesu ni "Mwokozi wa ulimwengu." Yesu alikuwa tayari kulala kwao, kula nao na kuzungumza nao, hiyo ilikuwa tofauti na desturi ya Wayahudi. Wayahudi hawakupenda maisha ya Yesu kwani yalikuwa rahisi na ya kujichanganya na matabaka ya watu wasiowataka. Hata leo usiweke mipaka, kila binadamu anahitaji habari njema, na itasaidia Yesu aje upesi!

Yesu akamaliza kazi Yake nje ya Uyahudi. Alikuwa ametembea umbali mrefu kumfikia mtu mmoja tu, mwanamke mnyenyekevu Msamaria. Mwanamke huyu akawaambia wenzake katika kijiji kizima. Hata leo Yesu anakuita wewe uliye mmoja hata kama ni mtoto. Yesu hakurudi Galilaya. Watu wa Galilaya walikuwa wagumu kuamini, wakisema tunamjua huyu amezaliwa hapa kwetu, na ndugu Zake ni Yakobo

na Yuda, dada zake pia tunawajua! Ndugu Zake wenyewe walikuwa hawamwamini, hadi alipofufuka. Yesu akasema "nabii hapati heshima kwenye nchi yake" na "adui wa mtu ni watu wa nyumbani kwake."

Hata leo watu wa karibu nasi wakituambia tumfuate Mungu na kuacha njia zetu mbovu, tutilie maanani wala tusiwape wakati mgumu. Yesu alikuwa tayari kutumia muda Wake na mtu mmoja. Hata nasi tusiwe na ubaguzi wa kuthamini umati wa watu na kutojisikia kuwahudumia watu wachache. Tusipendelee watu wa aina fulani tu kwa kuwa ni watu wa kabila letu, bali tuwahudumie watu wote ili wapate wokovu. Yesu alipopaa mbinguni Filipo, Yohana na Petro waliingia Samaria wakikumbuka siku zao na Yesu alivyoonyesha upendo mwingi kwa watu hawa, nao wakaonyesha upendo ule ule wakawahubiria watu habari njema tena na tena. Wale wanaomwamini Mungu wasiwe na matabaka na kutenga watu fulani kwenye jumuiya. Kwani kila mtu ni mwanafunzi wa Yesu na mmishonari kama mwanamke Msamaria alivyokuwa. Tukumbuke Yesu ni maji ya uzima, na yeye anywaye maji ya uzima huwapa wengine pia.

*Wakati ubinafsi unakufa, kutakuwa na mwamko mkubwa wa matamanio ya wokovu wa wengine, - hamu ambayo itasababisha kufanyika kwa juhudi za kudumu katika kutenda mema. Kutakuwa na kupanda kando ya maji yote; na sala yenye msukumo na mkazo, na maombi ya kujitolea, yataingia mbinguni kwa niaba ya roho zinazoangamia.


------------------------

Maswali: Yesu alimfuata mtu mmoja tu Samaria, hii inakufundisha nini? Sikari ilikuwa wapi? Mwanamke Msamaria alimwuliza Yesu maswali gani? Mavuno ni mengi bali watenda kazi ni wachache, ina maana gani? Yesu ni maji ya uzima ina maana gani kwako leo? Yesu alivunjaje kuta za makabila?

**SIKU YA 207**
**(Julai 25)**

# Yohana awekwa kizimbani na kuuwawa.

**Yohana 3. Luka 3 na Yohana 4.**



Yohana aliendelea kuhubiri watu watubu, na akawaelekeza toba halisi wanayopaswa kufanya. Hakuacha kumwambia Herodi. Herode Antipasi mfalme wa Galilaya alimweka Yohana mbatizaji gerezani kwa vile Yohana alimwambia dhambi yake ya kuchukua mke wa kaka yake aitwaye Herodia haikuwa halali. Herode alipotaka kumwua aliogopa watu kwa vile walimheshimu na kumtambua Yohana kama nabii. Yohana aliishi maisha ya kujinyima, wakati ambao wengi wakati huo waliishi maisha ya anasa, yaliyofanya wasitafute ufalme wa Mungu.
Mke wa Herode alimchukia Yohana, na akataka kumwua, ila Herode alimweshimu Yohana kama mtumishi wa Mungu. Herode alikuwa na udhaifu wa kushindwa kusimamia haki, kama alivyokuwa mfalme Ahabu, na alikuwa na udhaifu wa kumsikiliza mkewe kuliko Mungu. kwa kumweka Yohana, Herode alitaka amweke nabii Yohana kwenye gereza lililo mbali na lililo kwenye milima ya Bahari iliyokufa ili asiendelee kumchukia mke wake wa bandia, yaani hakuwa na ndoa naye, bali aliishi naye kama kimada.

Yohana mbatizaji anawakilisha watu wanaompenda Mungu watakaopeleka ujumbe wa matayarisho kwa ujio wa Yesu mara ya pili. Hawa wanapaswa kuishi maisha rahisi ya kujikana nafsi, na utii kwa Mungu. Ili watu waokolewe, yawapasa waseme bila kuficha, wanayopasa kutenda. Kuwa mkuu katika ufalme wa mbinguni hakutokani na umashuhuri, kupendwa na watu au kuwa na mali, bali usafi wa moyo na kujikabidhi kwa Mungu. Yohana mbatizaji alipata tunu ya kushiriki mateso ya Yesu, ili kutuokoa sisi wanadamu. Kila anayemfuata Yesu hupata mateso. Mfano wake umekuwa faraja kwa wengi waliopata mateso baadaye. Mungu alitoa mlango wa kutokea kwa Henoka, na Eliya walioenda minguni bila kuonja mauti. Hao

hawakuwa bora kuliko wengine walioteswa, bali Mungu katika hekima Yake aliona afanye vile, hivyo tukazane kwenda mbinguni ili tujue sababu za kutofautisha hatima! Katika yote twapaswa kumtumaini Yeye.

Yesu aliposikia Yohana amewekwa kizimbani alienda Samaria. Yohana mbatizaji maskini hakuelewa kwa nini jambo hili limetokea na huku alikuwa anamfanyia kazi Yesu kwa moyo wake wote. Mashaka yakamwingia. Akajihoji kama Yesu ni Masihi kweli. Kumbuka pia Yohana alikuwa binamu wa Yesu. Basi Yohana alituma wanafunzi wawili kumwuliza "Wewe Ndiye Masihi au tumngojee mwingine?" Yesu akawaambia wale waliotumwa Kwake warudi kwa Yohana na kumwambia yote wanayoona na kusikia kwake "vipofu waona, viwete watembea, viziwi wanasikia, wenye ukoma wanatakaswa, wafu wanafufuliwa, na masikini wanahubiriwa habari njema."

Wanafunzi wa Yohana wakaenda kwa furaha kumpa matumaini Yohana tena. Kisha Yesu akawaambia watu waliokuwa pale kuhusu sehemu ya Yohana kwenye kazi ya Mungu. Yesu akawauliza walitoka makwao kumtazama Yohana mbatizaji, naye kweli ni zaidi ya nabii maana alitabiriwa kuwa mjumbe wa kutengeneza njia ya Masihi "hajaondokea mtu katika uzao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana, walakini aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye. Kuanzia siku zile za Yohana ufalme wa Mungu ulipatikana kwa nguvu." Yohana alikuwa mashuhuri, hata watu wa juu walimjia. Ni rahisi umaarufu kuingia kichwani mwa mtu, na kumpa mtu kiburi, ila si Yohana.

Yohana alikuwa tayari kumshuhudia Yesu kwa hali na mali, katika umasikini na katika kifo. Watu walimchochea kwamba mbona Yesu anapata jina kuliko yeye na wala hamsaidii atoke, hapa gerezani? Naye aliwaambia wasimweke yeye maanani kuliko YESU, maana yeye alimtayarishia njia Yesu, kama vile mshenga amsaidiavyo bwana harusi kuoa au kupata mke. Yesu Ndiye BWANA Harusi, na yeye ni mshenga na anafurahi ajabu, anapoona mambo yanaenda sawa kwa Bwana harusi wake. Na yuko tayari akipotea ili macho ya watu yajikite kwa BWANA. Maneno haya yaliendelea kumpa Yohana, mtumishi wa Mungu faraja.

Herode alimwacha Yohana gerezani kwa muda, ili kupitisha wakati ili kumuimarisha Yohana kiroho. Japo alikatishwa tamaa, Yohana alikuwa mwaminifu kwa Mungu hadi mwisho. Siku moja Herodi alifanya siku kuu ya kuzaliwa kwake na walipokuwa wakiendelea kunywa pombe, binti yake Herodia, alicheza mbele ya watu, na kumpendeza Herode, naye akaahidi kwa kiapo kwamba atampa chochote atakachoomba, hata ikiwa nusu ya ufalme wake. Ni makosa kutoa ahadi za namna hii, maana zaweza kumfunga mtu kwenye pingu za uovu.

Basi yule binti wa miaka mdogo alienda kwa mama yake na kumwuliza aombe zawadi gani kwa mfalme. Mama yake akamwambia aombe kichwa cha Yohana mbatizaje kwenye sinia, kwa kuwa 'anawakosesha raha' kwa vile aliwaambia dhambi yao. Mfalme akasikitika kwa viapo vile vya ulevi na visivyo na hekima alivyovitoa kwa yule mtoto. Lakini akitaka kuwafurahisha watu na kutunza viapo vyake aliamuru mbele ya watu kuwa askari waende kumkata kichwa Yohana mle

gerezani na kukileta kwenye sinia. Wale wageni wangesimama dede na kupinga jambo hilo kamwe lisingefanyika. Lakini hilo lilishindikana kwa sababu walikuwa waoga na kisha ulevi ulikuwa umetanda vichwani mwao, wasiweze kuwa na akili bora au maamuzi bora.

Jambo hili lilifanyika, na yule msichana alikibeba kile kichwa kwa mama yake. Kwa mtu mwenye mawazo timamu na bora, ingekuwa tuzo, kupata nusu ya ufalme, kuliko kichwa cha mtu na damu zake kwenye sinia la chakula. Ni Mambo ya kutisha dhambi ikituingia na pale tunapoacha njia ya Mungu; chuki au wivu wetu huwa mkubwa na tunakuwa tayari kutumika maovuni bila kufikiri. Wanafunzi wa Yohana waliposikia kiongozi wao ameuawa walienda kuchukua maiti na kuzika kisha wakampasha Yesu habari. Hatujui Kwa nini mambo mabaya haya yalimpata mtumishi wa Mungu, au Kwa nini Mungu aliruhusu yatokee, ila kuna siku Mungu atatufumbulia fumbo hili. Kwa sasa tumtumaini Mungu na kujua kwamba Yeye si dhalimu, yaani daima ni Mwenye haki, ila kwasababu ya mapambano na ufalme wa Shetani, kutoka Shetani aasi mbinguni, Mungu amekuwa akijaribu kadri inavyowezekana kuleta amani, bila ya kukiuka Sheria Yake ya Upendo. Mungu ilibidi aweke kanuni za vita na kuziheshimu kama Mungu atunzaye agano. Sheria hizi zinajumuisha kumpa mtu na Shetani uhuru wa uchaguzi, bila ya kumwangamiza Shetani na malaika zake mpaka siku ile ya hukumu, ambapo jopo la binadamu litakapokaa na kushuhudia kwenye sayari zote na ulimwengu wa Mungu usio na kikomo kwamba Mungu ni ametumia Haki, na ni UPENDO. (jury duty), kwamba Mungu ni upendo! Wazungu wanasema What a day ! What a day! Yaani siku ya ajabu kiasi gani hiyo jamani! 1 Wakorintho 4:9, Soma fungu hili na kutafakari kuhusu hii tamasha au onyesho la video kwenye malimwengu yote! Wanadamu watakuwa majaji wa malaika!

Twaambiwa Yohana hakufanya miujiza watu waliyoiona, ila kila alichosema kuhusu Yesu kilikuwa ile Kweli tupu. Watoto na watu wazima leo, twaweza tusiwe na karama ya miujiza kama Petro au Paulo, ila tuwaambie watu Habari za Yesu za Kweli, ili wasipotee, bali wawe na uzima wa milele. Baadaye Herode alianza kupata hofu aliposikia habari za Yesu akihubiri akasema "Yohana niliyemkata kichwa amefufuka." Aliishi maisha ya hofu yasiyo na furaha, kutokana na kumfanyia mtumishi wa Mungu uovu.

Kutoka Samaria alikwenda Kana, pale alipobadilisha maji kuwa divai. Kila mtu alitaka kumwona aliposikia amekuja pale. Kulikuwa na diwani mmoja ambaye mwanawe alikuwa anaumwa na alifurahi aliposikia Yesu amekuja. Akamwendea akamsihi ashuke na kumponya mwanawe kwa maana alikuwa anakaribia kufa. Wazazi wanakuwa na huzuni mtoto wao anapoumwa. Mara nyingi wanaona ingekuwa heri wao wenyewe waumwe kuliko mtoto wao. Alipofika alikuta Yesu ni mtu wa kawaida tu, asiye na mavazi ya fahari, akajiuliza huyu kweli atanisaidia? Ila kwa vile alishafika pale, akaona wacha tu amwambie Yesu shida yake.

Yesu alitambua mawazo na mashaka aliyonayo kuhusu uwezo Wake akasema "Msipoona ishara na maajabu hamtaamini kabisa?" Wasamaria wa Sikari, walikuwa na imani kwa Yesu kuliko Wayahudi. Yule baba akagundua kwamba Yesu si mtu wa kawaida, na akaomba Yesu aende naye kwake. Yesu akamwagiza yule diwani aende

zake tu nyumbani kwake maana mtoto yu hai. Mtu yule alisadiki aliloambiwa na Yesu naye akashika njia kwenda nyumbani Kana, umbali wa kilomita 16 hivi, na alipokuwa njiani, watumishi walimlaki na kumwambia, mtoto wake yu hai, maana amepona. Yule Diwani akauliza ni majira gani alipona? Nao wakamwambia saa saba homa ilimwacha. Diwani huyu akajua ndiyo saa ile ile aliyoambiwa na Yesu "mtoto wako yu hai."

Basi huyu Diwani akamwamini Yesu, yeye na wote wa nyumbani mwake. Hii ikawa ishara ya pili Yesu aliyofanya. Tukumbuke, yeye asiyemtegemea Mungu na kutafuta kumjua, ana ugonjwa zaidi ya wagonjwa wale tunaowajua. Mara nyingi tunamtafuta Mungu na kusali tunapokuwa na shida, au tukitaka vitu. Yesu anataka kutupa kitu cha thamani zaidi ya vitu vyote. Naye anatupokea tulivyo, bila ya ubaguzi au kutuhukumu kwa maswali "Kwangu ajaye yoyote sitamtupa kamwe". Anataka tuwe marafiki Zake wa karibu, tunayezungumza Naye si wakati mambo yakiharibika tu kama tunavyoita zima moto kutuliza janga, bali masaa 24/7 ya siku. Twaweza kuamini ahadi Zake bila woga, na kwamba anajibu maombi. Tumwombe atubariki, tuamini tutatendewa tuombayo, na tumshukuru kwa yote, tukijua pale atakidhi mahitaji yetu, na kutuondolea vihofu.

Kifo cha Yohana mbatizaji kiliwatia moyo na faraja, mamilioni waaminifu, walipouwawa. Wale wote waliokufa kwa Jina la Yesu, kwenye magereza ya giza na ukiwa, kwa mapanga, moto na ukatili mwingi wa aina zote uzoefu wa Yohana umewafariji kwamba hawajasahauliwa na Mungu. Shetani alitaka kumpa Yesu huzuni kwa kumwua Yohana. Yesu alipata huzuni, naye pia akauwawa na mwovu. Ila tukumbuke wote wanaomfuata Mungu, watapata mateso ya aina fulani toka kwa mwovu. Eliya na Henoka waliopaa hawakuwa bora kuliko binamu ya Yesu Yohana mbatizaji.

Yesu alikuwa amekuja Galilaya alipenda watu Wake na akataka wapate habari njema. Ila hao, walikuwa na mioyo migumu. Hata leo tunatahadharishwa tusiwe na mioyo migumu, tukingoja ishara na maajabu tu, bali tufanye maamuzi kumchagua Yesu.

*Tunapaswa kufanya makongamano ya maombi, tukimwomba Bwana afungue njia ili Ukweli upate kuingia katika ngome ambazo Shetani ameweka kiti chake cha enzi, na kuondoa kivuli alichotupa katika njia ya wale ambao anatafuta kuwadanganya na kuwaangamiza.

----------------------------

Maswali: Diwani alikuwa na shida gani? Kwa nini Yohana aliwekwa kizimbani na kuuwawa? Je ungekuwa mvulana au msichana wa miaka 14 ungeomba zawadi gani? Je msichana wa miaka 14 amekomaa kiasi cha kuwajibika kuchuja matakwa ya mama yake au mapenzi ya Mungu? Kwa nini tumwamini Mungu hata tusipoona ishara na maajabu? Fundisho gani twapata kutokana na maisha ya Yohana Mbatizaji?

**SIKU 208**
**(Julai 26)**

# Yesu ananza kazi kwao Nazareti alipolelewa

**Luka 4. Mathayo 4.**



Yesu akasikia kwamba Yohana amefungwa, Naye akaenda Galilaya, katika kijiji cha Nazareti na kisha Kapernaumu mji wa pwani karibu na Zabloni na Naftali, ili litimie Neno lililonenwa na nabii Isaya akisema "Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, Njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa. Watu wote waliokaa katika giza wameona mwanga mkuu. Nao waliokaa katika nchi na uvuli wa mauti, Mwanga umewazukia." Kuanzia hapo alianza kuhubiri na kusema "Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia."

Yesu aliweka wazi kwamba ufalme Wake si wa duniani au wa vita. Alisema ufalme Wake ni wa upendo na yoyote aweza kujiunga nao. Aliwaambia watu wasijali kuhusu Warumi wanaowatawala. Kwani hiyo siyo shida ya binadamu kubwa, bali ni dhambi. Wakitubu, na kumfuata Yeye, wamejitengenezea maisha kuwa mazuri milele. Yale mambo ya kutawalaliwa na Warumi ni ya muda, hivyo wawapende tu na mambo yote yatakuwa sawa. Akasema wakitumwa nao kuchukua mzigo maili moja, waende maili mbili. Wakiagizwa kubeba koti lao, wawabebee na mashati yao pia. Mtu yoyote mwenye roho ngumu akiona unampenda, moyo wake unalainika.
Yesu akawaambia siku moja falme za dunia zitapita na ufalme wa Mungu wa upendo utamiliki milele. Bustani ya Edeni iliyopotea itarudishwa kama paradiso. Chuki itaondolewa kwani kila mtu atampenda mwingine kwa upendo wa dhati. Mafundisho haya yalikuwa mageni kwao, bali yalienea kama moto kwenye nyasi kavu. Watu walijua hajainuka mhubiri kama huyu. Sumaku ya Roho wa Mungu

iliwavuta wakajua kwamba ni BWANA. Nao wakamsikiliza na kuuliza maswali. Wengine wakamfuata kila alipokwenda, furaha yao ikawa ile isiyo na kifani.

Japo hawasemi sana kuhusu watoto au wanawake waliomfuata, maana siku zile hawakuandika yote, watoto wengi na wanawake walimfuata hata wakamhudumia pia, wakishukuru mema mengi ya ajabu aliyowatendea. Wengine waume zao walifanya ofisi ya Herode. Walishangaa hekima na ufumbuzi aliowapa kwa kila tatizo lao. Hakuna ambalo hakuweza kutatua. Wakashangaa maarifa Yake ya ajabu, japo hakwenda chuoni, au shule za marabi. Walichopenda kupita yote ni kule kujali kwake kila mtu. Haijalishi ni nani alienda kuzungumza naye, mwanamume mtoto, mzee, mwanamke. Alijichanganya na watu, akaonyesha kujali na upendo, kisha akawasaidia, na baadaye aliwaambia wamfuate. Hata nasi leo twapasa kufuata mfano huu, tusimwambie mtu amfuate Yesu ila akiwa na shida hatupo tayari kumsaidia, bali tunapenda jamaa zetu tu.

Yesu alimjali sana Yohana mbatizaji kama nabii wa Mungu, aishiye katika dunia yenye shida. Mungu huwapa vijiti vya kupokezana wale wanaofanya kazi shambani Mwake. Pale mmoja anapoishia kukimbia, wengine wanaendelea kupeleka nuru hiyo maana mtume Paulo au Yohana hawapo tena. Basi tuepuke kuona wivu kwamba maisha ya mtenda kazi wa Mungu fulani, au rafiki yetu, yana raha na fahari kushinda yetu. Kuwa kwake kwenye nafasi hakumaanishi atakuwa na nafasi ya juu zaidi kwenye ufalme wa mbinguni. Tuwe na roho kama ya Yohana mbatizaji, aliyejishusha, ili kazi ya Mungu isonge mbele. Hata mitume, nao walifanya kazi na kuachia wengine. Leo kijiti ni chetu wewe na mimi. Tukimbie kwa saburi na imani, na endapo tutalala usingizi wa mauti tuwape wengine waendelee ili siku moja turithi lile tumaini linalobubujika daima.

Aliendelea kufikiri majukumu yaliyo mbele Yake, akijifunza na kuzungumza na Baba Yake kila siku hata kabla ya majogoo kuwika. Alitaka awape watu waliopondeka mioyo matumaini ya uzima wa milele, asaidie wenye shida na kuponya wagonjwa. Zaidi ya yote alitaka aonyeshe dunia nzima upendo mkubwa wa Mungu. Alitaka amwite kila mtu "Njoo kwa Mungu! ILI usaidiwe, na kusamehewa dhambi." Hata wewe leo, atakupa maisha mapya, ukimwamini. Aliendelea na ule ujumbe wa habari hizi njema za kuwaambia watu "Ufalme wa mbinguni umekuja." Sehemu nyingi alizoenda alikuta Yohana mbatizaji amemtayarishia njia. Wengi walipomsikia sauti Yake na huruma Zake, walipata matumaini, amani na furaha moyoni. Alinukuu Maandiko ya manabii mara zote, akionyesha Maandiko ni mamlaka ya mwisho na sauti ya Mungu aliye Hai.

Alijua kifo kichungu cha msalaba kinamngoja; na alijua wale watu anaotaka kuwaokoa na kuwapa mema watamkana na kukataa upendo wake. Alijua mwishowe watamsulubisha msalabani. Licha ya haya yote, alinuia kufanya mapenzi ya Babaye na kutimiza kila alichomwagiza. Aliendelea kuzungumza na Baba Yake, na kumwomba nguvu na ujasiri kila siku ili aweze kufanya mapenzi Yake. Hata leo Mungu anapenda kuishi nasi na kutupa furaha ya kweli, ila hawezi kutulazimisha, kumwamini na kumtumaini. Huo ni uchaguzi wetu. Mungu ni wa Kweli, na Yupo, na yapasa tuchague njia Yake tukitaka tuokolewe. Yeye anataka atuokoe kila mmoja

wetu, ila anaheshimu uchaguzi wako; hawezi kukulazimisha au kukushurutisha umpende.

Wakati wa majaribu na katika kipindi chote cha maisha ya Yesu, Ibilisi alitaka amwache Baba wa mbinguni ili mpango wa wokovu usifanikiwe. Yesu hakutaka kutumia Uungu Wake kwa faida Yake Mwenyewe. Ibilisi alikuwa tayari kunukuu Maandiko kwa makosa, na kutaka Yesu ajitupe ili aangamie au watu wamfuate kama mtu wa mazingaombwe. Yesu aliona mpango wa wokovu ndiyo muhimu na si kumridhisha mwovu shauku Zake. Yesu hakutaka watu wamfuate eti kwa vile amewatendea miujiza, bali wamfuate kwa imani kwa kuwa Yeye aweza kuwaokoa kutoka katika dhambi zao na kwamba wanataka wawe na urafiki Naye. Yesu akiwa amechoka na mwenye kiu na njaa; Ibilisi alitaka amwabudu ili ampe milki zote sasa za dunia kwa mara moja! Yesu hakusahau Maandiko na kwamba ni Yeye Ndiye aliyeumba milki hizi zote.

Yesu alipoanza kazi alihubiri kwenye masinagogi na watu wengi wakamfuata ili kumsikiliza, maana hawakuwa wamesikia mahubiri mazuri kama yale maisha yao yote. Alizungumza kama mtu aliyekuwa na mamlaka, uwezo na hekima. Hata leo ukiwa na shida au mashaka moyoni mwako, jifunze kumtumaini. Kwa njia hiyo utakuwa na uhakika wa kujua la kufanya, ikiwa ni kwa jema au baya. Kumwamini Yesu kunatupa amani na usalama ambao binadamu yoyote hawezi kutupatia. Watu watashangaa kwamba japo u mtoto, na huna elimu ya shahada kubwa, maisha yako yametulia, yana furaha, na unajua kujibu watu maneno ya kufariji.
Wengine wasiompenda walitaka apate shida na serikali ya Rumi iliyotawala wakati huo. Basi wakamtungia mabaya mengi na kuwa na nia moja tu, ya kufanya huduma yake ikome.

*Kila mtu Anaweza Kuombea Roho — Sio wote walioitwa kufanya kazi binafsi katika maeneo ya nchi za kigeni, lakini wote wanaweza kufanya kitu kwa maombi yao na zawadi zao kusaidia kazi ya umishonari.

*Siku hizi za maandalizi zilikuwa siku za uchunguzi wa moyo kwa kina. Wanafunzi walihisi hitaji lao la kiroho na wakalia kwa Bwana kwa ajili ya upako mtakatifu ambaye angewafaa kwa kazi ya kuokoa roho. Hawakuomba baraka kwao wenyewe tu. Walielemewa na mzigo wa kuongoa roho. Walitambua kwamba injili inapaswa kupelekwa ulimwenguni, nao wakadai nguvu ambayo Kristo alikuwa ameahidi.


*MUNGU anataka vijana wenye kiasi, wenye kujistahi, wanyenyekevu, watulivu, wenye akili timamu, na wanaume wenye umri wa kukomaa, ambao wana msawaziko wa kanuni (balansi), ambao wanaweza kuomba na kuongea, ambao watainuka mbele ya wazee ili kuonyesha heshima kwao, na kuwatendea waliowazidi kwa kuwaheshimu.
---------------------------

Maswali: Kwa nini Yesu alizungumza kama mtu Mwenye mamlaka na uwezo? Kumwamini Yesu kunatusaidia nini? Yesu alianza kazi miji gani? Kwa nini watu walishangaa kwa mafundisho Yake?

**SIKU YA 209**
**(Julai 27)**

# Yesu akataliwa kwao Nazareti.

**Luka 4**



Yesu alipoenda Nazareti baada ya kushinda majaribu, na harusi ya Kana aliendа Nazareti alipolelewa, na kama ilivyokuwa desturi Yake aliendа kwenye sinagogi kuabudu. Watu hapa walimjua; alikuwa amerudi nyumbani, na wengi walikuwa wamesikia kuhusu miujiza aliyoifanya Mahali pengine, ila watu wana kawaida ya kudharau cha kwao. Mithali moja ya kiswahili yasema, akujuaye hakuthamini.
Walimpa Yesu asome Maandiko, na akapewa chuo cha nabii Isaya. Alipokifungua chuo cha kitabu hicho, alitafuta mahali palipoandikwa "Roho wa BWANA yu juu Yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri masikini habari njema. Amenituma, kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa." Yesu akakifunga kitabu kile na kumrudishia mtumishi wa hekalu na watu wote waliokuwa katika sinagogi wakamkazia macho. Yesu akawaambia "leo Maandiko yametimia masikioni mwenu." Wakastaajabu Maneno Yake kwamba yana maana gani.

Shetani akawapa mashaka na kiburi kuhusu maisha Yake, japo maisha Yake ya nuru yaliwashitaki. Wakauliza "siye mwana wa Yusufu huyu"; wakaulizana inakuwaje

mambo yote haya makubwa ya nabii Isaya anasema yanamhusu? Yeye akawambia mtaniambia bila shaka "tabibu jiponye nafsi yako" na mtaniuliza yote niliyotenda Kapernamu nitende hapa. Akawaambia hakuna nabii anayekubaliwa kwenye nchi yake, kwani walikuwa wajane wengi Israeli ila Eliya aliienda kwa mjane wa Sarepta katika nchi ya Sidoni, kulipokuwa na njaa ya miaka mitatu na nusu. Akasema tena wengi walikuwa na ukoma, ila Naamani wa Shamu ndiye alitakaswa.

Wale watu waliposikia hivi walijaa ghadhabu. Hawakumpa Roho wa Mungu nafasi ya kuwakatisha shauri kufuata ile njia ya Mungu. Walikasirika alipotaja watu wa mataifa kama Naamani au mjane. Wakasimama na kumtoa nje ya mji, wakimpeleka ukingo wa kilima wapate kumtupa chini afe. Ila alipotea kati yao kimiujiza, na kwenda Zake, maana muda Wake ulikuwa haujafika. Leo hii kuna wengi pia wanaotaka wahubiriwe yale wanayotaka. Wanaweza wasitake kuwaua kama Wayahudi, bali wanawasema vibaya na kuwachukia.

Tukumbuke, leo malaika wanalinda watoto na watu wazima wasiangamizwe na Ibilisi. Ni mbingu tu zitatueleza siku moja tulivyookolewa na mipango ya Shetani aliyetaka kutuangamiza. Yesu alikuwa tayari kuwasaidia, ila Shetani alikuwa amewakaba wamkatae, naye Yesu asingeweza kuwalazimisha. Aliondoka kwa huzuni kutoka sinagogi la nyumbani Kwake na kwenda Zake. Tukumbuke kiburi na mapokeo bila Ufunuo ni kitu kibaya. Lazima tujue elimu au maarifa yetu hayatatuokoa, bali Mungu Mweyewe katika mpango Wake wa wokovu wa Masihi Ndiye tumaini letu.
Kutoka Nazareti, akashuka Kapernaumu na kuwafundisha siku ya Sabato, wakashangaa. Na ndani ya sinagogi au kanisani, kulikuwa na mtu mwenye roho ya pepo mchafu, akalia kwa sauti kuu "Tuna nini Nawe, Yesu mnazareti? Umekuja kutuangamiza? Nakujua u nani, Mtakatifu wa Mungu." Alikiri yule ajenti wa Shetani kupitia kwa kinywa cha huyu mtu. Yesu akamkemea yule pepo "fumba kinywa chako umtoke." Pepo yule alimwangusha mtu huyu, na akamtoka bila kumdhuru. Watu wakashangaa, kwamba "awaamuru pepo wachafu kwa uwezo na nguvu, na hutoka." Habari hizi zikaenea.

Hata leo kuna mamilioni wenye mapepo duniani, ila kwa Jina la YESU yanatoka. Hebu yule mwenye pepo atafutiwe watu wenye imani, na kuombewa, na mtu huyu kwa Jina la Yesu mapepo watatoka. Mapepo huingia mara nyingi kwa mtu, au wazazi wa mtu, wanaporuhusu mambo fulani ya giza kwenye maisha yake au yao. Pepo hufanya kikao na mtu huyu, na kumkosesha raha na hata kumwangamiza. Mtu huyu lazima amkubali Yesu kwenye maisha Yake na kuacha maisha ya zamani. Asipofanya hivi, mapepo yakitoka, huwa yanarudi na kumtesa zaidi ya hapo awali. Yesu akiwafafanulia ukweli huu akilinganisha hali hiyo na mtu aliyefagia au kujaribu kuondoa matendo mabaya kwa uwezo wake. Basi kuondoa matendo mabaya tu bila kumwingiza Yesu mioyoni mwetu haisaidii. Maana tukijaribu kufagia matendo mabaya yatoke kwa uwezo wetu kama mafarisayo, moyo utajazwa na mambo mabaya zaidi.

Akatoka katika sinagogi akaenda nyumbani mwa Simoni Petro, ambaye mama mkwe wake alikuwa ameshikwa na homa kali. Wakamwomba Yesu amponye Naye, akaikemea ile homa na ikamwamcha mara hiyo hiyo. Mama huyu alipopona tu,

akaondoka na kuanza kuwahudumia wageni. Hii ilionyesha shukurani yake, na roho ya kutaka kutumika badala ya kutumikiwa. Hata leo ukiwa mgonjwa, ukipona tu anza kusaidia kazi ndogo ndogo nyumbani, bila kudeka au kujiendekeza. Jua lilipotua wengi wenye maradhi mbali mbali walikuwa wakingoja Sabato iishe, ili waje kwa Yesu, wasije wakahukumiwa na mafarisayo. Hawa walileta wagonjwa na Yesu akaweka mikono Yake juu ya kila mmoja na kuwaponya. Watu wengi waliponywa pepo, hawa walipiga kelele wakisema "Wewe u mwana wa Mungu." Akawakemea waache kunena."

Shetani anamjua Mungu vyema, maana aliumbwa naye, na aliishi naye mbinguni. Tofauti ni kuwa yeye hana imani na Mungu na hutenda maovu daima. Watu hawa wenye mapepo ilikuwa rahisi Kwake kuwaponya, kuliko wenye viburi au wanafiki kama mafarisayo waliofikiri hawana hitaji lolote. Waliyapindisha pindisha Maandiko na yakawa mizigo ya mawe kwa watu. Daima hawakuchoka kumfuata Yesu. Walitembea maili nyingi hapa na pale, milimani na mabondeni, wakaacha shughuli na familia zao, ili kuleta uchokozi, au ugomvi. Waliposhindwa, walirudia tena na tena. Kiburi na wivu ni dhambi mbaya, maana inatufanya tuone tuko sawa, na hatuhitaji kuponywa au badiliko lolote. Mtu mmoja amesema wale watu wasiosoma na wenye dhambi, uovu wao ni rahisi kuponywa, kuliko wale waliosoma au wanafiki, maana dhambi zao ni nzito na husitiriwa mahali ambapo hawahimizwi kuomba msamaha. Mfano mzuri ni nchi za Magharibi zinavyochanganya teknolojia na nguvu za giza, mara zingine inakuwa vigumu kuelewa ili maombi yatolewe ipasavyo, ukilinganisha na wachawi wanaoagua kwenye vijiji masikini huku wamevaa nguo zinazojulikana na watu wengi.

Yesu alitoka aende pasipokuwa na watu, ila makutano yalimtafuta na kufika Kwake, wakimzuia asiondoke kwao. Kila anayemlilia Mungu leo, hata asipozungumza kwa sauti, anasikiwa. Yesu akawaambia "imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia." Basi aliendelea kuhubiri katika masinagogi ya Galilaya. Kwake Yesu hakuna binadamu asiyekuwa na faida, au muhimu kuliko mwingine. Wote ni viumbe Vyake, na alitaka mema kwao. Aliwapa matumaini wale waliokata tamaa, na wale ambao watu hawakutegemea. Aliwatia moyo wasiojiweza, na waliojikuta wameangukia kwenye hila za Shetani akiwahakikishia kuwa Mungu aweza kuwabadilisha. Wale waliomwamini waligundua kwamba wanaweza kumkabidhi shida zao zote, na atawasaidia.

Alikaa Kapernaumu ya kuwatayarisha mioyo yao wampokee Yesu. Mafundisho ya Marabi yalikuwa baridi na yasiyo na upendo ila Yesu alikuwa akizungumza kwa uwezo, mamlaka, na upendo. Maneno Yake yalieleweka na watu wasiosoma na waliosoma. Hakufanya vitu ili ashangiliwe au kusifiwa, bali aliwaonea watu huruma, na akataka atimize mapenzi ya Baba Yake. Hakuna aliyefungwa asiweze kufunguliwa na Mungu leo. Sauti Yake ilipendwa na wote wenye shida, au waliohitaji kusaidiwa. Hakuna aliyeomba msaada akafukuzwa au kushushuliwa. Yesu alifurahi kila wakati mtu alipochagua uzima wa milele, na akasikitika watu walipokataa Njia ya Kweli na uzima.

Alitumia muda mwingi wa faragha kuomba na kutafakari Maandiko na akarudi

tena kufanya kazi. Yesu alichoka akifanya kazi usiku na mchana, ila hatusomi mahali panaposema aliugua, bali tunasoma panaposema alibeba magonjwa ya watu na udhaifu wao. Hata leo Anachukua magonjwa na udhaifu wetu.

*Fanya kazi miongoni mwa watu wa hali ya chini, masikini, na walioonewa. Tunapaswa kuwaombea na kuomba nao wale wanyonge, wasio na msaada ambao hawana nguvu ya kutawala hamu ya chakula au tamaa ya mwili imeiharibu. Jitihada za bidii na za kudumu lazima zifanyike kwa wokovu wa wale ambao mioyo yao imepata uamsho.


----------------------------

Maswali: Yesu alisoma Maneno gani kwenye sinagogi? Kwa nini watu walitaka wamtupe Yesu afe? Mapepo yalijuaje Yesu ni Mwana wa Mungu? Kwa nini Yesu alitumia muda mwingi kuomba?

**SIKU YA 210**
**(Julai 28)**

# Wavuvi waitwa tena kuwa wanafunzi.

**Luka 5.**



Makutano yakamsonga Yesu katika ziwa la Genesareti. Akaona vyombo vimekaa ziwani ila wavuvi hawamo ndani, bali wanaosha nyavu zao. Akaingia kwenye chombo cha Simoni Petro na akamwambia akipeleka pwani kidogo. Akawafundisha makutano akiketi kwenye chombo kile. Alipomaliza kuzungumza na watu alimwambia Petro "Tweka mpaka kilindini mkashushe nyavu zenu mvue samaki." Petro akashangaa, kwamba kumbe Yesu hajui wamesumbuka toka asubuhi na hawakupata kitu.

Wengi twajua hata leo mchana si wakati nzuri wa kuvua. Na Petro mvuvi aliyebobea alijua hili halina maana kabisa, ndipo akamwambia Yesu "BWANA mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha tusipate kitu." Ila kwa sababu Wewe Ndiye umetuamuru, tutafanya tu kwa vile ni Wewe. Hata leo kuna mengi Mungu anataka tufanye yasiyoleta maana au kueleweka kwetu, ila tujaribu kufanya kwa vile YEYE amesema, na tutashangaa. Tufanye, maana hekima na mahesabu Yake si ya kibinadamu, anakiuka kanuni za asili au maumbile, kwa vile Yeye ni Mwumbaji.

Petro alimheshimu Yesu ila hakuwa anamjua vizuri. Alikuwa na shauku ya kumpendeza au kumfurahisha maana alikuwa mtu mwema Kwake. Basi akatupa nyavu na akapata samaki wengi mpaka nyavu zikaanza kuchanika. Wakawapungia mkono wale wavuvi wenzao waliokuwa na ubia nao, waje haraka kuwasaidia. Wakajaza vyombo vyao vyote viwili samaki, hata vikataka kuzama. Simoni Petro akapata mwangaza tena kwamba Yesu ni nani. Akaanguka kwa unyenyekevu magotini pa Yesu akijua wazi wazi sasa kwamba Yesu ni BWANA wa viumbe. Akajiona hafai, pungufu na duni akalia "ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, BWANA." Japo alisema vile, alimshika miguu ya Yesu kwa nguvu, hakutaka kumwacha! Maana alishikwa na ushangao yeye na wote aliokuwa nao pamoja naye. Yakobo na Yohana wana wa Zebedayo ndiyo walikuwa na ubia pamoja na Petro na Andrea.
Yesu akamwambia Petro kwa upendo "usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu." Basi wavuvi wote hawa waliviacha vyombo vyao wakamfuata wawe wavuvi wa

watu milele zote. Kabla ya hapo walivua na kurudi kwao, ila sasa walikwenda wakijua wanalo jukumu zito. Wakajua kazi yao ni kuvua watu. Kumfuata Yesu ndiyo uamuzi mzito hawa wavuvi walifanya. Hata leo Yesu angali anatuita wewe na mimi, tumfuate. Je utaitika na kufungua moyo wako ili Yesu Kristo afanye makao moyoni mwako? Hakuna kikomo kwa kile mtu anaweza kufanya na kutenda kama amejitoa na kufungua moyo wake ili Roho Mtakatifu aingie ndani yake na tena kama amejitoa wakfu maisha yake kwa Yesu Kristo. Yesu alikuwa amezungumza na kuleta matumaini, faraja, hekima na amani kwa wavuvi hawa, ambao walibadilisha dunia nzima alipopaa mbinguni. Udhaifu waweza kuwa nguvu tukimtegemea Mungu na kumtumaini kama mitume walivyofanya.

Katika mji ule kulikuwa na mtu mwenye ukoma na akaja kwa Yesu kuomba aponywe na kutakaswa na ukoma. Yesu alinyosha mkono wake na kumgusa akisema "nataka takasika." Mara hiyo ukoma ukamtoka. Yesu akamkataza asiwaambie watu, ila aende akajionyeshe kwa makuhani, na kutoa sadaka ya kutakasika kama Musa alivyoamuru kuwa ushuhuda wake. Ila yule mtu hakufuata maelekezo akaenda akawaeleza wengine juu ya kupona kwake na habari zikazidi kuenea. Basi watu wengi wakakusanyika ili kumsikiliza na kuponywa. Baada ya hapo Yesu alijitenga kando na watu akaenda mahali ili asali. Alichukua muda mwingi kusali, na hili ni fundisho kwetu sote. Tusipitishe siku nzima au hata masaa kadhaa bila kusali. Maombi ya binafsi ndiyo siri ya ushindi, si maombi ya hadhara, japokuwa yana sehemu yake. Turudi madhabahuni, na tusali asubuhi na jioni, kama kwenye Biblia Kutoka 29:39, nasi japo hatutoi kafara, twapasa kufanya huu mwendelezo!

Ikawa siku zile alikuwa akifundisha nyumbani mwa Petro, na mafarisayo ambao walikuwa walimu wa sheria au torati walikuwa wameketi, wakitokea Galilaya kama wapelelezi. Hawa walikuwa watu wa umri mkubwa ukilinganisha na Yesu kijana wa miaka 30 tu. Hawa walimu na viongozi walitaka kumwona Yesu na kumsikiliza maana kila mtu alikuwa amezungumza kuhusu habari Zake. Walikuwa wakijiuliza mioyoni mwao, jinsi gani mtu huyu ambaye ni maskini au seremala aweza kufanya vitu walivyowasikia watu wakisimulia?

Yesu alipoanza kuzungumza, ikaonekana kama kuna vurugu. Na tazama watu wakaja wamemchukua mgonjwa wa kupooza kitandani wakitaka kumwingiza ndani ya nyumba mule Yesu alimo. Waliombeba walikosa nafasi ya kupita mlangoni kutokana na umati wa watu. Waliamua kutoboa dari na kumshusha yeye na kitanda chake katikati mbele ya Yesu. Hawa lazima walikuwa marafiki wakubwa na walitaka rafiki yao apone. Yesu alipomwona yule mtu alijua hitaji lake "ninakumtamkia msamaha wa dhambi" akasema "Ee rafiki, umesamehewa dhambi zako." Hata leo Yesu anatuambia Maneno haya matamu "Rafiki, umesamehewa dhambi zako zote." Wengi hata leo kutokana na kutenda dhambi, dhamira zao zinawashitaki na wamejawa na huzuni nyingi.

Wale waandishi wa mafarisayo waliposikia walianza kusemezana, Je ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Mungu peke Yake? Yesu akijua hoja zao, aliwauliza wanahojiana nini mioyoni mwao? Akasema "Lipi ni rahisi kusema? Umesamehewa dhambi zako, au ondoka uende?" Akawafahamisha "mpate kujua ya kwamba

Mwana Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi." Kisha akamwambia yule mgonjwa aondoke na kujitwika kitanda chake, naye akasimama mbele yao na kujitwika kitanda alicholalia akaenda zake nyumbani kwake huku akimtukuza Mungu. Mshangao uliwashika watu pale, na wakamtukuza Mungu, wakijawa hofu, wakasema "leo tumeona mambo ya ajabu."

Yesu aliwapumzisha watu na huzuni, mashaka, na maumivu. Aliwaambia "njoni Kwangu nyinyi nyote mnaolemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu mjifunze Kwangu, kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi." Maelfu walikuja Kwake akawaponya. Wengine waliokuwa maskini walipata faraja. Hakuuliza wanatoka wapi? Au wana dhambi gani, bali aliwashughulikia katika mahitaji yao. Aliwapa vyote walivyohitaji. Machozi ya maelfu yalifutwa, shida zikatatuliwa na huzuni zao zikatokomea. Kwenye vijiji vingi alimopita, hakukubakia na mgonjwa hata mmoja!
Basi hata leo katika udhaifu wowote tulio nao, tunaweza kumgeukia Yesu atusaidie. Katika majaribu tunayopata, tukimgeukia Yeye, tutapewa nguvu, na hekima za kuyastahimili yote. Tukimfuata Yeye atatuonyesha mapenzi Yake. Wengi kama mtu huyu aliyekuwa kitandani walikuwa wamejitwika fadhaa na misongo iliyowakosesha furaha. Kila walipojaribu kuishi kulingana na mapokeo ya binadamu au desturi, mizigo yao ikawa mizito zaidi. Leo Mungu anataka tumpe mashaka yetu na mizigo yote, tumtumaini Yeye. Tukimweka Yeye kuwa namba moja, tutagundua ana njia mabilioni ambazo hatuzijui za kututatulia matatizo yetu. Shule Yake itatutoa kifungoni mwa mapokeo yasiyo Kweli, tabia mbovu, na mafundisho potovu tuliojifunza toka kwa adui.


Yesu daima alikuwa na amani moyoni Mwake, hata pale penye hatari au kukataliwa, hakuonyesha fadhaa. Alizijua changamoto za moyo wa mwanadamu, wala hakuna mtu ambaye angeweza kumdanganya. Leo wengi wana fadhaa wakiogopa kumtumaini Yeye na kumkabidhi Yeye kila mzigo wao. Matatizo ya dunia hayawezi kutuharibu kama tutamwekea mizigo yetu. Tukijisalimisha Kwake, Yeye anachukua mizigo yetu. Ufalme wa mbinguni wa neema unaanza hapa hapa duniani tukimkabidhi yote na kumpokea Yeye atatupa ufalme wa utukufu Wake.
*Niliona kwamba kila ombi ambalo hutolewa kwa imani kutoka katika moyo mwaminifu litasikika juu kwa MUNGU na kujibiwa, na yule aliyetuma ombi atapata baraka wakati anapoihitaji sana, na mara nyingi majibu huzidi matarajio yake. Hakuna ombi la mtakatifu wa kweli linalopotea ikiwa limetumwa kwa imani kutoka katika moyo mkweli na mnyofu.
-----------------------------

Maswali: Kwa nini Petro alisema hatuwezi kuvua samaki? "Tangu sasa mtakuwa wavuvi wa watu" ina maana gani? Je umechukua muda kusali leo? Kwa nini Yesu ana uwezo wa kusamehe dhambi? Watu wenye mizigo waliambiwa nini na Yesu? Mtu aliyepooza, alisaidiwa na nani kupitia darini? Kukufuru, ni pamoja na kusamehe watu dhambi zao, eleza kwanini hatupaswi kuomba msamaha wa dhambi na kuungama kwa mwanadamu mwenzetu, hata akiwa kiongozi wa dini?

**SIKU YA 211**
**(Julai 29)**

# Mathayo aitwa awe mwanafunzi, na afanya karamu ya kuaga wenzake.

**Luka 5.**



Baada ya hapo alitoka na kumwona mtoza ushuru jina lake Lawi ameketi forodhani kwenye kibanda chake. Akamwambia "nifuate", naye akaacha kibarua chake hapo hapo na kuondoka kumfuata Yesu. Hakujiuliza maswali ofisi iliyokuwa inampa utajiri ataiacha na nani. Huenda alikuwa amechoka maisha ya kuishi kwa ulaghai na rushwa. Japo alijua anafanya uamuzi mwema, alijua maisha yangekuwa magumu. Alijua angeanza kutembea kwa miguu badala ya gari la ngamia, kuishi nyikani badala ya nyumba kubwa. Alikubali kujitoa mhanga kuwa mwanafunzi wa Yesu. Alitambua pesa si kila kitu katika maisha. Je wewe ungeitwa leo, ukiwa na mali nyingi, kuwa mfuasi wa Yesu ungejibu nini?

Katika watu waliochukiwa wakati huo ni watoza ushuru. Watoza ushuru waliwakusanyia Warumi kodi. Warumi walikuwa wamewatawala kwa ukatili, hivyo watoza ushuru walionekana wasaliti. Watoza ushuru wengi walikuwa wabinafsi, na wakatili, wakiibia watu kwa kuwatoza zaidi ya walivyoambiwa na kisha kujiwekea vibindoni. Wapo watoza ushuru ambao hawakuwa waovu, ila jina lao liliharibiwa

na wale waovu. Lawi akafanya karamu kubwa nyumbani kwake kwa ajili ya Yesu. Alitumia karamu hiyo pia kuaga watoza ushuru wenzake, marafiki, ndugu na jamaa. Karamu ilisaidia Yesu kuwafikia wengine na neno la uzima. Mathayo huyu ndiye aliyeandika kitabu cha Mathayo. Yeye aliandika Maneno Yesu aliyosema, maana alimsikiliza na kumwona kwa macho Yake. Yesu alijua Mathayo angeandika kitabu na kuwajulisha wengi habari za wokovu wamchague Mungu.

Yasemekana Yuda na Mathayo ndiyo walikuwa wasomi kwa upande wa mitume. Wakiwa chakulani mafarisayo walikuja wakinung'unika kwamba wanafunzi wa Yesu wanakula chakula na watoza ushuru na wenye dhambi. Ndipo Yesu akawaambia "wenye afya hawana haja ya tabibu isipokuwa wagonjwa." Akimaanisha wanaojiona wenye dhambi wanajua wanamhitaji Mungu awasaidie, ila wale wanaojiona ni wenye haki, hawaoni haja ya kuwa na Mungu ili awasaidie. Maneno haya kwa undani, yamaanisha, hakuna mwenye haki hata mmoja. Yaani wale watu walikuwa na haki ya matendo yao wenyewe, si haki ambayo inatoka mbinguni. Haki ya binadamu hupingana na ufalme wa Mungu na humpeleka mtu upotevuni.

Wote tuko kwenye wodi ya wagonjwa hospitalini, tukiumwa ugonjwa wa dhambi. Kusema kwamba mimi nina kisukari, na yule ana presha, au mimi nina kikohozi na yule ana shida ya figo, hivyo mimi ni afadhali, ni kujidanganya. Tunahitaji tabibu na uponyaji wote wa Mwenyezi Mungu. Mitume hawakuwa wanafanana. Walitofautiana kitabia, na walitofautiana maeneo wanayotokea. Hauhitaji kufanana na mtu mwingine sana ili awe rafiki yako. Faida ya watu kutofautiana ni kuwa watawafikia watu tofauti na kuwaalika kwenye ufalme wa Mungu.

Basi mafarisayo wakaendelea kusema kwenye karamu ya Mathayo kwamba wanafunzi wa Yohana mbatizaji walifunga mara nyingi, na kuomba dua, na kadhalika wanafunzi wa mafarisayo; ila wanafunzi wa Yesu walikuwa wakila na kunywa. Yesu akawambia "Je mwaweza kuwafanya wafunge walioalikwa harusini Bwana harusi akiwapo pamoja nao? Lakini siku zinakuja watakapoondolewa Bwana arusi, ndipo watakapofunga siku zile." Aliwaambia hivi kama mithali au fumbo, kwamba hakuna atiaye kiraka kipya kwenye vazi kuu kuu, na kama akitia, lile vazi kuu kuu litapasuka tena. "Wala hakuna atiaye divai mpya katika viriba vikuukuu na kama akiweka, ile divai mpya itavipasua vile viriba, na divai yenyewe itamwagika. Mtu akiwa na divai mpya sharti kutiwa katika viriba vipya. Wala hakuna anywaye divai ya kale akatamani divai mpya; kwa kuwa ataona ile ya kale ndiyo njema." Alisema hivi akimaanisha mafundisho ya uzima Yesu aliyokuwa Nayo ni mapya, na yale ya mapokeo ya mafarisayo ni makuu kuu. Yale mafundisho Yake hayawezi kuchanganyika na ya mafarisayo bila kuleta matatizo.

Mitume walifuatana na Yesu, waliponya magonjwa, waliombea watu, na walihubiri. Watu wadogo hawa walijikuta, wamekuwa matabibu na wahubiri wakuu kwa ajili ya kuwa na Yesu. Leo kuna watu wanahitaji huduma hizo pia. Wewe ni mwanafunzi wa Yesu, haijalishi umri wako. Mtu asiudharau utoto au ujana wako. Mpokee kwa moyo wako, na ufuate kile mitume walichofanya.

Hebu tusikilize Mitume wakijieleza kwa ufupi:
Andrea: Mimi nilikuwa mtume wa kwanza. Nilikuwa mvuvi. Niliposikia Yohana akisema Yesu ni Mwana-Kondoo wa Mungu na mkombozi, nilimfuata Yesu na baada ya siku moja, niliharakisha kumwita ndugu yangu Simoni Petro aje pia.
Simoni Petro: Mimi nilikuwa mvuvi, Yesu akaniita kuvua watu. Nilikuwa mtu asiye nadhifu, na hivyo ikawa kazi kweli kuwa mwanafunzi wa Yesu. Mara nyingi nilikuwa nasema vitu mbavyo si sawa. Wengine walisema naropoka bila kufikiri. Nafikiri kuna watu wengi wenye tabia kama yangu. Yesu alinivumilia, na kunibadilisha. Nilikuwa mwanafunzi wa kwanza kumhubiri Yesu alipofufuka na kufanya muujiza. Nilihubiria watu wa mataifa pia. Natajwa kwenye vitabu vya injili na Matendo kuliko mwanafunzi yoyote mwingine

Yakobo: Mimi na kaka yangu Yohana, tulikuwa na biashara ya kuvua. Na tulikuwa tunavua na baba yetu Zebedayo. Tuliacha biashara hii na kumfuata Yesu. Mimi na kaka yangu tulijulikana kama wana wa ngurumo. Ukisoma injili utagundua hilo. Siku moja tukiwa kwenye kijiji cha Samaria tulitaka Yesu aamuru moto ushuke na kuwaangamiza watu kwa vile walikataa tusikae kwao. Yohana na Petro na mimi tulikuwa karibu zaidi na Yesu kuliko wanafunzi wengine. Tulikuwa Naye Gethsemane, na pale mlimani ambako alibadilika kwa mng'aro na nguo Zake zikimeremeta sana. Mimi ndiyo nilikuwa mtume wa kwanza kufa kwa ajili ya Jina la Yesu. Niliuwawa na mfalme Herode.

Yohana: Kama kaka yangu Yakobo alivyosema tulikuwa watu wa hasira, hatimaye Yesu alitupa jina 'wana wa ngurumo'. Mama yetu aliitwa Salome na alikuwa na ujamaa na Mariamu mama wa Yesu. Yesu alipokuwa msalabani, alinipa jukumu la kumtunza mama Yake. Niliishi miaka mingi, baada ya Yesu kurudi mbinguni, nikashuhudia kanisa kukua katika nchi zile za Mediteranean. Mtawala mmoja alinitia kifungoni kwenye kisiwa cha Patmo Uturuki. Nikiwa kule niliandika kitabu cha Ufunuo. Najulikana kama mtume wa upendo, kwani nilikazia upendo wa Mungu kwenye maandishi yangu.

Filipo: Kazi yangu inayojulikana ni kuwatambulisha watu kwa Yesu. Nilimtambulisha rafiki yangu Nathaniel, kwa Yesu. Niliwatambulisha pia kwa Yesu, Wayunani waliokuja kuhiji.
Nathanieli: Filipo alinipeleka kwa Yesu. Jina langu jingine ni Batolomeo. Kwa kuwa nilijua vyema uovu unaotendeka Nazareti, nilimuuliza kwa mshangao Filipo wa kuwa "kuna kitu chema chaweza kutoka mle?" Yesu alinihakikishia kuwa aliniona kabla sijaja nilipokuwa chini ya mkuyu. Hilo lilinifanya niamini kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu. Yesu, alisema sina hila, Mwisraeli kweli-kweli, na alishangaa kwamba haikunichukua muda mrefu kuamini. Akaniahidi nitaona maajabu zaidi ya hayo.
Mathayo: Watu huniita Lawi, ila nimeitwa na watu majina mengi kwa kuwa kazi yangu ya utoza ushuru ilikuwa inawachukiza. Niliwatoza watu ushuru zaidi na kujiwekea kibindoni. Watoza ushuru wengi tulikuwa na tabia hii. Nilichukiwa, na kuonekana mwenye dhambi. Siku Moja Yesu alikuja ofisini mwangu na kuniambia nimfuate. Nikafanya karamu kwa ajili ya Yesu na kualika marafiki zangu. Nimeandika kitabu cha Mathayo.

Tomaso: Mimi naitwa Tomaso mwenye mashaka. Ila nilikuwa tayari kwenda na Yesu popote na hata kufa Naye. Sikuwepo Yesu alipojitokeza kwa mitume baada ya kufufuka ila wengine walimwona. Mimi sikuamini tarifa za kufufuka Kwake. Nilitaka nizione na kugusa alama Zake za misumari ili niamini. Ila Yesu alipojitokeza kwetu, nilianguka kwenye miguu Yake na kumsujudu papo hapo Bwana wangu na Mwokozi wangu.
Yakobo: Usinichanganye na Yakobo kaka wa Yohana.
Simoni: Naitwa Simoni Zealoti, maana nilitaka serikali ya Rumi ipinduliwe. Sikupenda watutawale. Nilikuwa mkereketwa na mpigania uhuru. Kama siku hizi ningeitwa gaidi,. Sijulikani sana ila tulimfuata Yesu kwa uaminifu. Baada ya Yesu kufufuka tulienda kuhubiri injili.
Thadayo: Jina langu jingine ni Yuda, usinichanganye na Yuda Iskarioti ambaye alimwuza Yesu. Sikujulikana sana.
Yuda Iskariote: Mimi ndiye niliyemsaliti Yesu. Mitume wote walitoka Galilaya, isipokuwa mimi. Kwa kweli nilikuwa nampenda Yesu, na alikuwa mwema kwangu mno, ila tamaa yangu kwa pesa ilikuwa kubwa zaidi kwangu. Nilikuwa mtunza hazina wa kundi letu, nikajiwekea kibindoni vingine, nikifikiri ni haki yangu kwa vile nilikuwa na uwezo kiakili zaidi. Mimi ndiye nilikuwa najua mambo zaidi ya wote. Nilitaka nimtumie Yesu ili niwe mashuhuri. Yeye hakuniita ila nilijipeleka. Japo niliishi na Yesu miaka mitatu na nusu sikutaka kubadilika. Nilimwuza Yesu nikijua hana hatia, nikafikiri kwa vile ana uwezo, angejiokoa. Nilifikiri hii ingemharakisha kujitawaza kuwa mfalme, nami ningeambulia kazi yenye cheo kwenye serikali hiyo. Nilishtuka kwamba anaenda kusulubiwa bila ya kuponyoka. Hapo ndiyo niliona nimesaliti damu isiyo na hatia. Viongozi wa kanisa waliniponza baadaye wakanikimbia, wangenisaidia hata kuungama, nami sikuona sababu ya kuungama, kwani kiburi changu kiliniponza, nikafa siku moja na Yesu kwenye mti kama yeye, ila mimi kwa kujinyonga.

*Tukimwuliza, MUNGU atajibu -Ni sehemu ya mpango wa MUNGU kutupatia, kwa kujibu maombi ya imani, yale ambayo hangetoa ikiwa hatukuomba.
------------------------------

Maswali: Mathayo aliacha nini alipomfuata Yesu? Je, wawezaje kufanya karamu ya kufikia watu na habari njema kwako? Mtume Nathanieli anajulikana kwa maneno gani ya kwenye Biblia? Kwa nini Yuda Iskariote hakubadilika tabia yake? Ungependa uwe mtume gani kati ya watu hawa? Toa sababu! Ni ahadi gani za BWANA zinatukumbusha kwamba maagizo yake yote ni kuwezesha? Mfano-Zaburi 32:8 "Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; nitakushauri, jicho Langu likikutazama."

Zaburi 34:11 Njoni, enyi wana, nisikilizeni, Nami nitawafundisha kumcha BWANA. Kumb 28:1 Itakuwa utakaposikia sauti ya Bwana, Mungu wako, kwa bidii, kutunza na kufanya maagizo Yake yote nikuagizayo leo, ndipo Bwana, Mungu wako, atakapokutukuza. juu ya mataifa yote ya dunia. "Hatua za mtu mwema zaimarishwa na Bwana Naye aipenda njia Yake". Zaburi 37:23.
Yoshua 1:9 "Iweni hodari na moyo wa ushujaa; msiogope wala msifadhaike; kwa kuwa Bwana Mungu wako yu pamoja nawe kila uendako."

**SIKU YA 212.**
**(Julai 30)**

# Mambo ya kufanya siku ya Sabato.

**Luka 6 , Luka 13 na Yohana 5.**

Ikawa siku moja ya Sabato Yesu na wanafunzi waliokuwa na njaa walipita kwenye mashamba ya ngano na wakawa wakivunja masuke na kuyapukusa ili wapate ngano waile. Jambo hili liliruhusiwa mtu akiwa na njaa, ila tu asibebe hicho chakula akaenda nacho kwake. Baadhi ya mafarisayo wakasema mbona mnafanya lisilo la halali siku ya Sabato? Wakiwa na maana kwamba wanafunzi wanavuna mazao siku ya Sabato. Yesu akasema "hamkusoma kwamba Daudi alipokuwa na njaa aliomba mikate ya wonyesho kwenye nyumba ya Mungu na akala japo hakuwa kuhani?" Akawaambia Mwana wa Adamu Ndiye BWANA wa Sabato, na kwamba Sabato ilifanyika kwa ajili ya watu na si watu kwa ajili ya Sabato.

Siku nyingine ya Sabato Yesu aliingia kwenye sinagogi ili afundishe na huko alikuwako mtu mwenye kupooza mkono wa kuume. Mkono wake ulikuwa mwembamba kupita mwingine kwa ajili ya kukosa mazoezi. Kutokana na hali hiyo huyu mtu asingeweza kupata kibarua, kuoga vizuri au kufanya shughuli yoyote. Madaktari walijaribu kumsaidia wakashindwa, hivyo ikabidi awe 'omba omba'. Kila alikopita watoto walimkodolea macho, na kunong'onezana huku wakimteta. Waandishi na mafarisayo walimvizia ili waone kama atamponya siku ya Sabato. Yesu akiwa na uweza wa kusoma mawazo yao, alimwambia aliyepooza aondoke na kusimama kisha akawauliza "Je ni halali siku ya Sabato kutenda mema au mabaya? kuponya roho au kuangamiza?" Akawakazia macho na kumwambia yule mgonjwa anyoshe mkono, nao ukawa mzima tena. Wayahudi wakaja, na uchungu moyoni wakishauriana wao kwa wao wamdhuru Yesu kwa njia gani. Yesu akaondoka akaenda mlimani akikesha na kuomba usiku kucha.

Mafarisayo hawakulipenda jambo hili. Ila siku nyingine Kristo akiwa nyumbani kwa mtu wakati walipokuwa wakila. Yesu akawauliza kama kondoo au mifugo yao ingetumbukia kisimani siku ya Sabato je, wangeacha kuitoa? Kwa sababu ya unafiki wao, watu hawa walinyamaza kimya huku wakijua jibu lake. Yesu akawaambia kama wamengemtoa kondoo kwenye shimo, basi binadamu ni wa muhimu zaidi kutolewa kwenye shimo hata kuzidi hao wanyama wanaowathamini. Yesu hakumaanisha tunatakiwa kuzipanga kazi hizi za kuponya kwenye ratiba ya kila Sabato, la! Alichomaanisha ni kwamba tuzifanye tu pale zinapokuja kwa dharura. Mtu anayeponywa siku ya Sabato ni kama aliyetolewa kifungoni. Na kumpa mtu nafuu siku hiyo ni jambo lililo jema maana kimsingi Sabato ni siku ya habari njema. Hata leo mahospitalini na kwenye huduma zingine muhimu kazi hufanyika siku ya Sabato na hilo ni jambo jema. Kinachotakiwa kwa watu kama hao ni kuhakikisha wanafanyiana zamu, ili wapate nafasi ya kuhudhuria ibada. Yesu aliwaona Wayahudi kuwa ni wanafiki na watu wanaopenda kushika sheria bila upendo wa Mungu. Walishughulikia matendo ya nje ili kulinda hadhi yao, bali nia na mawazo yao

yalijaa uovu.  Kushika tu sheria bila kusukumwa na upendo hakuwezi kutufikisha mbinguni. Matendo ya sheria yanapaswa kuwa matunda ya kumjua Mungu. Kristo alisema kwa matunda yao mtawatambua. Ni muhimu kama watoto wa Mungu, kuwa na huruma kwa wale wanaopata maumivu ya mwili au ya roho.

Siku ya Sabato Mungu aliagiza isiwe ya kufanya kazi bali kukaribiana na Mungu na kufanya ushirika wa kuabudu pamoja. Watu wapaswa wafurahie siku hii, maana Mungu aliumba siku sita na kupumzika ya saba. Hebu tufanye siku hii kuwa ya furaha na kumwabudu Mungu katika uzuri wa utakatifu Wake. Sabato ni siku njema ya kufanya mambo mema. Si siku ya kujifanyia anasa zetu kama Isaya 58 inavyotushauri, bali kufanya yampendezayo Mungu; tukichukua muda kutafakari Maandiko ambayo ndiyo usalama wetu, na kumsifu Mungu kwa uumbaji Wake na yote anayotusaidia siku kwa siku.

Sabato ni zaka ya siku, yaani siku iliyotengwa kuwa na mahusiano na Mungu wetu, na Baba yetu. Japo Mungu hahitaji mapumziko, lakini anajua sisi tunahitaji mapumziko.  Sisi tunahitaji kupumzika maana miili yetu huchoka. Twahitaji mapumziko ya kulala usiku masaa manane kila siku na siku moja ya wiki ya kuacha kazi zetu. Marafiki katika jimbo la Kalifonia waliniambia wao wameamua siku ya Sabato kujengea watu nyumba wakitoka kanisani. Wengine wameacha kuja kanisani siku ya Sabato kwa kwenda kuwapa pole waliofiwa, japo mgonjwa alifariki Jumatatu. Hawa waliendelea na shughuli zao juma nzima wasitoe pole.  Ila ile siku ya BWANA wetu ya Sabato, ndiyo wapo au wanakuwa tayari waivunje na kuitumia kuongezea mida yao ya utume, ili wasitumie zile zao. Tujitahidi mambo mengi kufanya au kutenda kwa siku zetu sita, ila ya saba ni ya mahusiano yetu na Mungu. Isipokuwa unapeleka ibada huko! Kwa machache, ni kwamba yale unayoweza kufanya siku nyingine fanya ili uwe na nafasi na BWANA Muumba siku ya Sabato.

Wayahudi waliweka sheria nyingi za Sabato. Yasemekana zilifika sheria 1,521. Kama siku ya kutahiri mtoto ya nane ikiangukia Sabato walimtahiri mtoto, ambao ni upasuaji wa mwili. Yesu alitaka watunze Sabato, ila isiwe kongwa, kwamba mtu hawezi kutolewa kwenye maumivu, janga, huzuni au dharura fulani siku ile, mpaka kesho yake. Wayahudi pale pale wakaanza kujawa chuki na ghadhabu, japo ilikuwa ni Sabato, wakaanza kufikiria mawazo ya kuua.

Siku nyingine akiwa kwenye sinagogi akisoma Maandiko alimwona mwanamke aliyekuwa amepinda mgongo yaani mwenye kibyongo alitokezea. Mwanamke huyu alikuwa na pepo wa udhaifu kwa miaka 18. Hakuna tabibu aliyeweza kumsaidia naye hakuweza kujinyosha. Matabibu wana ukomo katika utendaji wao. Kile wanachojua na wanachoweza kufanya kuokoa maisha  ni machache mno kati ya mabilioni ya maarifa yahusuyo mwili. Basi Yesu alimwona mwanamke huyu na kumwonea huruma. Aliona mafarisayo wakiangalia atakalofanya siku ya Sabato, ila hili halikumfanya asitende mema, au kile kilicho halali. Yesu akamponya mwanamke yule.

Hata leo wengi watatuangalia kama tunaenda mema au mabaya! Basi Yesu, alimshika mwanamke kichwani na kumwambia “umefunguliwa katika udhaifu

wako." Mgongo ukakunjuka, na akafurahi, japo viongozi wa sinagogi walichukia wakisema, "Kuna siku sita zifaazo kuponya watu" mbona unamponya siku ya Sabato? Hawa walisahau kwamba ingekuwa wao, mambo ya ulema ni magumu na mazito, wasingetaka waje kesho yake ndiyo wapewe afueni! Mama huyu hakuweza kufanya kazi zake, alikuwa anategemea wengine kumpatia riziki yake ya kila siku, na alijawa na huzuni. Pengine alikuwa na watoto au wajukuu akashindwa kuwahudumia, na siku ile aliwekwa huru. Hata hivyo Mungu hatendi kazi kwa kuponya! Huzungumza tu na mambo yanakuwa! Mwingine alimwambia sema Neno moja tu, na roho ya mtumishi wangu itapona! Je kuna kutoa jasho katika kusema Neno moja tu?


*MUNGU husikia maombi. Mkiniomba chochote kwa Jina Langu, Nitafanya." Tena anasema, "Mtu yeyote Akinitumikia, Baba Yangu atamheshimu." Yohana 14:14;Yohana 12:26. Ikiwa tutaishi kulingana na Neno Lake, kila ahadi ya thamani aliyotoa itatimizwa kwetu. Sisi hatustahili rehema Yake, lakini tunapojitoa Kwake, Yeye hutupokea. Atafanya kazi kwaajili yetu na kupitia wale wanaomfuata.
-----------------------------

Maswali: Mitume walipokula masuke ya ngano waliambiwaje na mafarisayo? Mwanamke wa kisa hiki alikuwa na shida gani miaka 18? Mwanamke huyu aliponywaje? Mtu wa safura alisaidiwaje? Ni mambo gani ya kufanya Sabato na kutofanya? Soma kitabu kinachoitwa Tumaini la vizazi vyote, kuhusu maisha ya Yesu, nawe utabarikiwa sana.

**SIKU YA 213**
**(Julai 31)**

# Kuponya siku ya Sabato.

**Luka 6, 13 na Yohana 5.**



Siku moja Yesu akitembea karibu na kisima cha Bethesda, karibu na mlango wa mauzo ya kondoo, kule Yerusalemu, alimwona mtu aliyepooza. Watu wengi wenye vilema kama viziwi, vipofu na viwete, walikuja hapa kwani waliamini kuna malaika anayetibua maji, na yakitibuka mtu atakayeingia kwa mara ya kwanza ataponywa na maradhi au shida yake. Yesu alimwona mtu aliyekuwa na kilema cha kupooza kwa miaka 38 akiwa pale. Akijua macho ya mafarisayo yanamtazama na angeweza kuepuka macho ya viongozi wa kidini hawa ambao walikuwa wameacha dini na kuwa wapepelezi, alimwuliza yule kilema "Je wataka kupona."

Mtu huyu alipata tumaini kidogo, akifikiri mwanamume huyu ambaye ni kijana mwenye nguvu, anayeniuliza atanisaidia kunitukumbukiza kwenye maji pale yatakapotibuka. Basi yule mtu akamwangalia Yesu akisema "Sina mtu wa kuniweka kwenye maji yakitibuka ili nipate kuponywa, kila mara yakitibuka mwingine ananiwahi kuingia." Yesu akamwambia "amka na chukua godoro lako, na utembee." Mtu huyu alinyanyuka papo hapo na kubeba kigodoro chake na kutembea. Haya yalitokea siku ya Sabato. Wayahudi walipomwona anafurahi na kutoa ushuhuda, badala ya kufurahi naye wakamlaumu kwa nini anabeba virago vyake siku ile ya Sabato. Wakataka aweleze ni nani aliyemponya, naye hakujua yule aliyemponya, kwa vile alikuwa ameshaondoka.

Baadaye Yesu alimwona yule mtu aliyemponya kwenye hekalu akamwambia aache kufanya dhambi, la sivyo jambo baya zaidi litampata. Ndipo yule mtu akatambua ni Yesu Ndiye aliyemponya, naye akaenda kuwaambia Wayahudi, naye akiwa hajui hila yao. Wayahudi wakamsumbua Yesu wakimtafuta ili wamwue, eti kwa kuwa alisema Mungu ni Baba Yake. Mgonjwa huyu wa miaka 38 aliishi maisha magumu, asiweze kutembea, kutafuta riziki, kwenda kuoga, kufua au hata kwenda msalani

mwenyewe. Jaribu kufikiri yote ambayo huko nyuma hakuweza kufanya na sasa aliweza kuyafanya. Je, hilo halikuwa jambo linalostahili kufurahia? Je! Tunafurahi na wale ambao wamepata muujiza, au kufanikiwa kwa namna fulani? Kama la! Twapasa kufanya hivyo!

Yesu aliwaeleza Mwana hawezi kufanya kitu bila idhini ya Babaye mbinguni. Akawaambia Baba Yake anafufua wafu, Naye pia kwa vile ni Mwana afanya afanyayo Baba Yake. Akawaambia Mwana amepewa kuhukumu, hivyo yeye asiyemheshimu Mwana atakuwa pia hamheshimu Baba. Shetani aliwafunga macho, wasiwe wanyenyekevu kwa Yesu. Hawakujua kwamba Yeye Ndiye mhukumu wa haki na Kweli, atakayewahukumu wanadamu, na badala yake wao ndiyo wakaanza kumhukumu! Akawaambia mtu yoyote atakayesikia Neno Lake Naye aliyemtuma yaani Mwenyezi Mungu, yuna uzima wa milele.
Hata leo, uzima wa Milele ni kusikia Neno la Mungu na kulitii. Wayahudi waliwawekea watu sheria nyingi, wakafanya Sabato kuwa mzigo au kongwa badala ya furaha. Wayahudi hawakuweza kuwasha taa, au mambo mengine hata madogo siku ya Sabato. Siku ya Sabato ikifika walikuwa wakiwategemea watu wengine wa mataifa wawafanyie. Waliamini kuwa ni Wayahudi pekee watakaookolewa. Yesu angeweza kumponya mtu huyu siku nyingine, ila alichagua kumponya siku ya Sabato kusudi awaonyeshe watu Wake namna sahihi ya kuheshimu na kuitunza Sabato kwa utukufu wa Mungu. Katika kufafanua Yesu akaelezea nafasi Yake katika Uungu jambo lililowakasirisha Wayahudi wakidhani ya kuwa alikuwa anakufuru. Ilikuwa vigumu kuwapendeza watu wa taifa Lake kwa lolote.

Yesu akawaambia "Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani Yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima." Kila unabii, hubiri, kurasa au kisa cha Agano la Kale vyote vilikuwa vinamshuhudia Kristo. Maagano haya mawili yanakamilishana! Moja ni mwendelelezo wa jingine. Kazi za kuacha kufanya siku za Sabato ni zile za kila siku za kutafuta riziki au anasa zetu. Viongozi wa sinagogi waliaibika, maana walijua kwamba hata wao kama wengekuwa na tatizo; wasingetaka Yesu angoje hadi kesho yake ili kuwatatulia tatizo hilo. Pamoja na kuwa viongozi hawakufurahia kuponywa kwa mgonjwa yule, walikuwako wengine walioshangilia kuponywa kwake.

Yesu aliwaangalia watu waliokuwa wakilalamika kuhusu mtu ameponywa Sabato na kusema "wanafiki nyinyi, mnamfungua ngombe wenu asubuhi aende kula au kunywa maji, japokuwa ni Sabato. Na huyu mwanamke binti wa Mungu, amekuwa akisumbuka miaka 18, Je haikumpasa kufunguliwa kifungo hiki kwa kuponywa siku ya Sabato?" Mkuu wa sinagogi aliona aibu, na watu wengine walipigwa butwaa kwa uponyaji uliofanyika.

Wayahudi walikuwa na mtazamo mbaya kuhusu Sabato. Walidhani Mungu aliumba Sabato ili wanadamu waitumikie. Yesu akawaambia Sabato iliumbwa kwa ajili ya mwanadamu na si mwanadamu kwa ajili ya Sabato. Yesu akasema 'Yeye' Ndiye BWANA wa Sabato na hivyo anajua ni kitu gani bora kufanya siku ya Sabato. Aliposema hivi lazima walishtuka, maana tafsiri yake ilikuwa "Mimi hapa, Ndiye

niliumba Sabato, na Mimi ndiyo nina amri ya kusema itunzwe namna gani, na si mwanadamu!" Ni vyema kila mtu ajue kwamba Yesu Ndiye Neno aliyeumba dunia kwa siku sita, na katika siku ya ya saba akaumba Sabato; hivyo ana mamlaka ya Sabato. Yesu hakuvunja Sabato, aliitunza vyema, bali alitaka kuondoa unafiki uliopo katika utunzaji wa Sabato. Yeye Ndiye Aliyelitamka Neno, analijua lote, na bado akawa analitafakari kila siku, sembuse sisi tusio na ufahamu mzuri?

Hakuna mgonjwa aliyekuja Kwake, akayebaki jinsi ile ile bila kumponya. Na hakuna marehemu ambaye watu walikuja kumwomba msaada awasaide, ambaye alimwacha bila kumfufua. Yaonekana kama vile kila mtu aliyekutana Naye alifufuka! Kwani hata alipokutana na msafara wa mazishi wa kijana wa Naini, alileta uzima! Watu waliokuja Kwake wakiwa na shida waliondoka na furaha tele. Mungu hakuumba Sabato kwa ajili ya Wayahudi kama watu wengine walivyofikiri. Fikiria, Myahudi wa kwanza alikuja baada ya miaka maelfu ya uumbaji. Kutunza Sabato kulianza juma la kwanza la uumbaji, mara baada ya Adamu na Hawa kuumbwa. Hivyo Sabato ilikuwepo kabla ya kuwepo kwa taifa la Kiyahudi miaka mingi nyuma. Kutunza Sabato kusijikite tu kwenye yale tunayofanya na yale tusiyotakiwa kuyafanya bali ijikite katika mpango wa Mungu wa furaha na neema. Kuwa wakarimu, kutenda mema, kuwaweka huru wafungwa! Kamwe Yesu hakukanusha Sabato, bali alichotaka kutupilia mbali ni jinsi ya kuiadhimisha. Sabato si mzigo, bali ni furaha ya neema ya Yesu kutupumzisha na shughuli za kila siku ili tuwe na mahusiano Naye na kupumzisha michoko yetu. Jitahidi siku hiyo usifikirie shuguli za wiki iliyopita!

Yesu aliposema kwamba Baba Yake afanya kazi hata Sabato, ndipo walipoanza kupata mawazo ya kumwua. Walidai kuwa hatunzi Sabato na anamwita Mungu Baba Yake, wasijue kuwa Yeye kweli ni Mungu. Watu hawa walikuwa tayari kutunza amri ya nne, hata kama wakivunja ya sita ya kuua. Dai hili walilileta siku ile walipomsulubisha Yesu. Kila mtu awe na tahadhari, kwani mara nyingine mtu aweza kuingia dini mbovu ambayo humfanya atie mkazo kwenye sheria fulani, na kusahau, rehema na neema ya Mungu. Mtu anayemkataa Kristo, na kutosikia maneno Yake; Maneno yale ya uzima ndiyo yatamhukumu.

*Unapomwomba Bwana akusaidie, Mtukuze Mwokozi wako kwa kuamini kwamba unapokea baraka Yake. Nguvu zote, hekima yote, ziko chini ya mamlaka yetu. Tunachopaswa ni kuomba tu.

------------------------

Maswali: Mungu alitenga siku ya Sabato baada ya uumbaji kwa ajili ya nini? Wawezaje kujua siku gani hasa ni Sabato? Mambo ya kufanya siku ya Sabato ni yapi? Kwa nini viongozi wa sinagogi waliaibika? Mtu aliyeugua miaka 38 aliambiwa nini na Yesu?

**SIKU YA 214.**
**(Agosti 1)**

# Mlango wa kuingia mbinguni ni Mwembamba.

**Luka 13**

Akipita mijini na vijijini kufundisha, katika safari yake kwenda Yerusalemu, mtu mmoja akamwuliza Je BWANA watu wanaookolewa kwenda mbinguni ni wachache au wengi? Yesu akamwambia "jitahidini kuingia katika mlango mwembamba kwa maana nawaambia wengi watataka kuingia wasiweze. Wakati mwenye nyumba atakaposimama kufunga mlango, nanyi mkaanza kusimama nje na kuubisha mlango, mkisema, Ee BWANA tufungulie, Yeye atajibu na kuwaambia siwajui mtokako; ndipo mtakapoanza kusema, tulikula na kunywa pamoja nawe, tulifundisha katika njia zetu."

"Naye atasema nawaambia siwajui mtokako, ondokeni Kwangu ninyi nyote mtendao maovu. Ndipo kutakuwa na kilio na kusaga meno, mtakapomwona Ibrahimu, Isaka na Yakobo na manabii wote katika ufalme wa Mungu, nanyi wenyewe mmetupwa nje. Nao watakuja watu kutoka mashariki na magharibi na toka kaskazini na kusini nao wataketi chakulani katika ufalme wa Mungu. Na tazama wa kwanza watakuwa wa mwisho na wa mwisho watakuwa wa kwanza." Wengi wanataka kuingia mbinguni bali matendo yao hayalingani na kauli zao. Mtu aliyepania kwenda mbinguni, ni lazima ajitoe mhanga, na kupania kuushinda ubinafsi, na kuepuka kufanya vitu vinavyotufurahisha sisi na kuwaumiza wengine.

Yapasa tujisalimishe kwa asilimia mia moja na kujikana nafsi. Hii ndiyo maana ya kuingia kupitia mlango mwembamba. Ni kufanya vile ambavyo japo vinakuwa vigumu kuvifanya; huwa ni mfereji wa uzima wa milele na furaha kwetu, kwa BABA wa mbinguni, na kwa wenzetu. Je leo uko tayari kuweka Neno la Mungu moyoni mwako, na katika matendo yako? Juu ya swali kuwa wangapi wataokolewa, na wangapi watapotea, aliwaambia jambo hilo lisiwasumbue sana. Mungu haokoi watu kwa vile ni watoto wa Ibrahimu, bali huokoa kwa jinsi watu wanavyomwamini na kumtumaini Yeye. Yaani wanapoona hitaji lao la msaada.

Yesu aliwaambia baadaye njia ya mbinguni ni nyembamba, isiyo na urembo kama lami, maua au nakshi. Ila ile ya kwenda motoni ni pana, yenye lami na rahisi kuipita. Je wewe unapenda maisha ya namna gani? Maisha ya njia nyembamba au pana? Hili ni swali muhimu tunalopaswa kujiuliza kila siku. Maana kila siku tupo barabarani, tukikabiliwa na maamuzi ya kupita njia pana au nyembamba. Lazima tuwe wasema kweli, hata kama tutapata adhabu shuleni au nyumbani. Lazima kuchukua muda kusaidia wenye mahitaji, tukianzia na wazazi na ndugu zetu. Haya yote ni maamuzi ya kusafiri njia nyembamba.

Njia pana inaenda motoni, na njia nyembamba au mlango mwembamba ndiyo inaenda uzimani. Njia pana inachukua tabia zote mbaya. Ni pana ya kutosha kuchukua kila kitu, iwe ni kuiba, kusema uongo, kupoteza mida, kusengenya,

kutukana watu, kutoheshimu wazazi, kutaja Jina la Mungu bure, kuwa na wivu, kuwa na chuki, kunywa pombe na vileo vingine, kucheza dansi, kuangalia mikanda na Televisheni potofu, kuimba nyimbo za ovyo ovyo, uchawi, unafiki, kiburi, uchafu wa ngono, kutosamehe watu na uchafu au takataka zote.

Lazima tuwe waangalifu, ili tuweze kuokolewa, maana Wayahudi wangepata mtu anajitukuza, wangempokea kirahisi maana walipenda sana mambo ya kujikweza, ila Yesu alizungumzia mambo ya kujishusha na kuwasaidia wenye mahitaji na kujikana nafsi ili wawe daima kwenye ile njia nyembamba. Hata leo wengi, ikiwepo na wale wafanyao kazi makanisani kwa kuajiriwa au kujitolea, wanamkana Mungu kwa kutunza mapokeo yao na siyo kutenda Neno la Mungu. Wanaishi maisha ya fahari, na kusahau kwamba hiyo ndiyo njia pana.

Kusaidia watu wenye mahitaji kwenye nchi zetu masikini ni muhimu. Msaada unapaswa uanzie kwa ndugu zetu, jumuiya ya waumini na jirani zetu wote. Hebu tujiulize imani tuliyonayo na na jinsi tunavyomjua Yesu. Je twampenda kwa vile baba na mama wanampenda? Je twampenda kwa sababu ni mapokeo? Mbinguni hatuendi tukiwa kwenye mbeleko ya mzazi. Kila mtoto anazaliwa akiwa hana kitu na hamjui Mungu, yaani pagani na inabidi aje apate imani na ajenge msimamo wake wa binafsi.

Saa ile mafarisayo kadha wa kadha walimjia wakimwogopesha kwamba “Toka hapa uende mahali pengine kwa sababu Herode anataka kukua.” Naye akasema “Nendeni mkamwambie yule mbweha, Tazama leo na kesho natoa pepo na kuponya magonjwa, hawezi kunizuia siku ya tatu nakamilika.” Herodi alijulikana kwa sifa na jina lile la kuua watu. Yesu akaelezea kwamba ni lazima kifo Chake kitokee Yerusalemu kama manabii wengine na siyo Galilaya.

Baadaye aliwaambia watu ukialikwa harusini usikae viti vya mbele akaja aliyewaalika na kukwambia, toka kitini, mpishe huyu sasa hivi, na kwa aibu ikabidi uende viti vya nyuma. Bali kaa nyumba na aliyekualika akija na akuambie “rafiki yangu, njoo huku mbele zaidi; ndipo utakapokuwa na heshima mbele ya wote walioketi pamoja naye. Ukijipeleka juu utashushwa na ukinyenyekezwa utapandishwa

Akawaambia ukiandaa chakula usiwaite rafiki zako au ndugu zako au jirani zako wenye mali, wasije wakalipiza kukualika ukapata malipo; bali ualike walemavu, viwete, vipofu nawe utakuwa na baraka kwa Mwenyezi Mungu kwa kulipwa ufufuo wa haki. Hii inatokea sana mahali ninapoishi leo, maana watu hupeana zawadi na marafiki zao, kwa kulipizana hisani, yaani kwa utaratibu wa nipe nikupe. Wakati wa siku kuu ya Krismasi wengine wanasema “nilimpa sweta zuri, yeye amenipa saa ya plastiki ya China ambayo ni bei ya chini!”. Familia moja hutumia wastani wa dola 400 kwa zawadi, watu hujawa na msongo wa kuchagua aina za zawadi, na jinsi ya kupata pesa ya kulipia hizi zawadi. Tumwombe Mungu tusijiingize katika desturi za namna hii, tukiwa na zawadi tutoe kwa moyo, tusipokuwa nayo, kuna siku Mungu atatupa, tusiwe na kisebusebu na kihoro papo hapo. Yaani tunatamani tuwe kama wengine, lakina hatutamani wakati huo huo!

Yesu baadaye akasisitiza ukitaka kumfuata Yeye, lazima uhesabu gharama. Alisema mtu anayejenga mnara lazima ahesabu gharama, au anayetuma jeshi ili kupigana, lazima atathmini. Kumfuata Yeye au njia ya Mungu, yabidi unuie, siku kwa siku na kuomba nguvu toka Kwake.

*MUNGU ana mbingu iliyojaa mibaraka ambayo anataka kuwapa wale ambao wanatafuta kwa bidii msaada ule ambao Bwana peke Yake Ndiye anaweza kutoa
---------------------------

Maswali: 'Mlango mwembamba kuingia mbinguni' una maana gani? Je unapenda kusafiri njia pana au nyembamba? Kwa nini kukaa viti vya nyuma kanisani si jambo zuri? Kwa nini watu wengi hupenda viti vya mbele mpirani? Mtu akifanya karamu awaite nani? Wangapi wataokolewa, na wangapi watapotea? Ni watu gani watakaolia na kusaga meno? Yawezekanaje wa kwanza akawa wa mwisho na wa mwisho wa kwanza?

**SIKU YA 215.**
**(Agosti 2)**

# Mlima wa baraka-Heri, chumvi, taa.

**Luka 6, Mathayo 5-7.**



Yesu alipochukua muda kuomba usiku mzima, ilipofika asubuhi, alianza kuchagua wanafunzi Wake. Daima alitaka kuwa na BABA wa mbinguni kuomba uongozi wa kila hatua aliyochukua. Hawa wanafunzi walipojifunza toka Kwake, walitumwa wawili wawili kwenda kuwaambia wengine, ndipo waliitwa mitume. Hata kulipokuwa mchana aliwaita wanafunzi wake, na kuchagua kumi na wawili miongoni mwao, Simoni Petro, Andrea, Yakobo, Yohana, Filipo, Nathanieli aliyeitwa Bartolomayo, Mathayo aitwaye Lawi, Tomaso aitwaye pacha, Yakobo wa Alfayo, Simoni Zealoti au mkananayo, Yuda wa Yakobo au Tadayo (Lebeusi), na Yuda Iskariote msaliti.

Alichagua watu 12 kutembea Naye na kuwafundisha ili waende kote kote na kufundisha wengine dunia nzima. Siku hizi wanasema kufundisha 'walimu wa walimu'. Wanafunzi wengine alikuwa amewaita, awali, ila aliwaita tena na kuongeza wengine. Tunajua machache kuhusu mitume hawa. Kwa mfano tunajua wengine kama Petro na Yohana walikuwa wazungumzaji, na waandishi hivyo tumepata kuwaelewa zaidi ya wengine. Akashuka pamoja nao na kusimama kwenye tambarare.

Yesu alipowaona makutano alipanda mlimani na alipokwisha kuketi wanafunzi Wake walimjia, Naye akafumbua kinywa Chake na kuwafundisha mambo ambayo

yaligusa kila sehemu ya maisha ya binadamu katika safari ya mbinguni. Luka asema Yesu aliponya watu pia siku ile. Hubiri hili lilikuwa kama utangulizi na ufunguzi kwa wanafunzi kuanza kazi yao rasmi, au kusimika huduma Yake. Yesu alitaka kuwaeleza ufalme wa mbinguni ni tofauti na yale wanayofikiria ya kutoa Warumi. Alitaka kuwaeleza ajenda ya kuja Kwake ulimwenguni. Bila kipaza sauti wote walimsikia vyema.

Chati ya Heri Nane
Heri walio maskini wa roho, maana ufalme wa mbinguni ni wao. (Kifungu cha 3)
Heri wenye upole maana hao wataimiliki nchi. (Kifungu cha 4)
Heri wenye huzuni, maana hao watafarijiwa. (Kifungu cha 5)
Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana watashibishwa. (Kifungu cha 6)
Heri wenye rehema maana hao watapata rehema. (Kifungu cha 7)
Heri wenye moyo safi maana hao watamwona Mungu. (Kifungu cha 8)
Heri wapatanishi maana hao wataitwa wana wa Mungu. (Kifungu cha 9)
Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki, maana ufalme wa mbinguni ni wao. (Kifungu cha 10)

Yesu alianza mahubiri Yake kwa kutamka Heri nane, kisha akazungumzia kwamba waumini ni chumvi, na taa. Chumvi haikai pamoja tu imerundikwa, bali inasambaa kwenye Chakula ili ilete tofauti au ladha. Kisha alichukua muda mwingi kukazia sheria, na kwamba alikuja kuitimiza, na si kuiondoa. Yesu alishika sheria zote alizozitoa! Hakuvunja sheria. Kumalizia mahubiri haya ya mlimani, Yesu alizungumza jinsi ya kuishi maisha kama Mkristo au muumini. Heri kwa Kiyunani ni Makarios. Nimesikia watu wengine wakijiita kwa jina hili la "Heri au Makarios." Heri hizi hazijitegemei zenyewe bali zinatakiwa zipokelewe nasi zote, ili zibariki watu.

Naye Yesu akanena Heri nane, au Baraka nane ikimaanisha "wana furaha walio…" au "Heri..." Yawezekana tusisikie furaha au baraka tunaposikia umaskini ukitajwa kama baraka. Tunapaswa tuondoe hisia hizi maana tumebarikiwa na Yesu katika hali yetu ya umaskini wa moyoni, au huzuni. Tumtafute kwa bidii tukijua Yeye atatupa utajiri na kicheko cha furaha. Yesu aliona wengi walioomba waponywe, wenye shida za namna zote. Huduma hii ilihitaji eneo lenye nafasi. Uwanja au eneo lililokuwepo lisingetosha watu wote hawa kukaa kwa utulivu ili wamsikilize. Wanafunzi Wake walimzunguka, makutano wakatafuta mahali pa kukaa, wamtazame na kumsikiliza pia.

Yesu akawaambia watu, siri kuu za kuwa na furaha ya Kweli ni kuwa inatokana na jinsi tunavyoishi maisha yetu mbele za Mungu. Yesu akaanza akisema: "Wamebarikiwa au wana furaha walio maskini wa roho, maana ufalme wa mbinguni ni wao." Ni wanyenyekevu wa mioyo ndiyo watakubali zawadi ya wokovu wa Mungu, maana wako tayari Mungu awafundishe. Wamebarikiwa au wanafuraha wenye huzuni; maana hao watafarijika. Alizungumza wenye huzuni za sonona kwa mawazo mengi yatokanayo na maisha ya dhiki na maumivu ya moyo vilivyozalishwa na dhambi. Hawa wakijua kwamba dhambi zao zinampa Yesu Huzuni watamruhusu Roho Mtakatifu awabadilishe.

Tukiwa wanyenyekevu hatutajali maneno makali ya watu, au tabia zao ngumu au mbovu. Tutakuwa na uvumilivu na Mungu atatuonyesha jinsi ya kuchukuliana nao. Wamebarikiwa au wana furaha wenye upole; maana hao watairithi nchi. Wamebarikiwa au wana furaha wenye njaa na kiu ya haki; Maana hao watashibishwa. Hawa wana njaa na wako tayari kulishwa Neno la Mungu. Neno la Mungu huwapa furaha na kuepuka majaribu ya Shetani. Wamebarikiwa au wanafuraha wenye rehema; Maana hao watashibishwa. Kuwa na rehema ni zaidi ya maneno, ni matendo yenye rehema pia.

Wamebarikiwa au wana furaha wenye moyo safi; Maana hao watamwona Mungu. Japo kujua mafundisho makuu ya imani ni muhimu, lakini watu huisoma roho safi ijidhihirishayo katika mwonekano wa nje, na kujua sisi tu wanafunzi wa Yesu Kweli. Watu hawa wanatunza mawazo safi, na kukataa kufikiri mambo machafu. Moyoni ndipo Patokapo yote masafi au machafu. Moyo ni mdanganyifu na una magonjwa ya kufisha, na hakuna aujuaye. Tumpe Yesu mioyo yetu leo ili aisafishe. Wamebarikiwa au wana furaha wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri ya kuteswa imerudiwa mara mbili, kwani Yesu alijua kwamba watu watateswa na kupata dhiki nyingi endapo wanachagua njia yake. Hata leo ukipata shida kwa kumchagua Mwenyezi Mungu upate faraja kwani kuna baraka. Mmebarikiwa au mnafuraha watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila Neno baya kwa uongo, kwa ajili Yangu. Furahini na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii kabla yenu. Tukipata shida au dhiki, au pale watu hawatuelewi kwa wema wetu au kumfuata Mungu, hatuna haja ya kuwa na hofu. Tusiwe na kinyongo au kutaka kuwalipiza watu mabaya; kwani hatimaye yote yatakuwa mema kwetu. Kinachojalisha ni upendo wa mbinguni. Tumpende Mungu na watu, nasi tutakuwa tumetimiza sheria yote.

Watu wengi walifikiri kwamba watu waliopata shida wamelaaniwa au wana bahati mbaya. Ila ufalme wa Mungu una maajabu ya vinyume mfano ajikwezaye atashushwa, pale tulipokuwa dhaifu ndiyo tuna nguvu au wa kwanza ndiye atakuwa wa mwisho. Watu wakashangaa mno kwani waliamimi furaha inakuja kwa kuwa tajiri, mashuhuri au kupata mamlaka. Akawaambia watu kwamba kupata heshima ya dunia haihusiani sana na furaha ya kumfuata Mungu.

Yesu akawambia wote wanaompenda Mungu ni chumvi ya ulimwengu yaani waleta maisha kuwa na ladha na msaada kwa watu, ila kama chumvi ikiharibika haifai kabisa ila itupwe na kukanywaga. Ili chumvi iwe na faida haipaswi kukaa peke yake, lazima ichanganyike na chakula, nasi pia lazima tuchanganyike na watu ili kuwavua waje kwa Yesu. Siku zile friji zilikuwa hazipo za kutunza vitu; na badala yake watu walitumia chumvi ili kukausha chakula kisiharibike. Bila Watu wanaompenda Mungu na kumtumikia dunia ingeharibikiwa. Ila wale wanaosema wanampenda Mungu, na hali matendo yao ni kinyume, ni chumvi isiyo na faida. Maana inatoa harufu au ina ladha mbaya.

Yesu hakuzungumza na madaktari, wanatheolojia, au watu wenye mamlaka makubwa, bali washiriki wa kawaida kama sisi. Hivyo leo, wewe ni chumvi, kisha u

nuru ya ulimwengu. Yaani maisha yetu mema ni taa au mwangaza wa kuwabariki watu wamjue Yesu. Yesu ndiyo ile Nuru kubwa, tusikosee na kufiriki sisi ndiyo nuru kubwa. Yeye ni kama jua, sisi tunaliakisi kama mwezi. Taa yetu ndogo yapaswa iunganishwe na Nuru yake kubwa. Baada ya kuunganishwa Naye, tusiifiche taa hii chini ya uvungu bali tuangazie wote ili wapate kuona matendo yetu na wamtukuze Baba yetu wa mbinguni na siyo sisi.


*Yesu Anawasilisha Maombi Yetu Yenye Maneno Mabovu na duni kwa Baba-Kila ombi la dhati husikika mbinguni. Linaweza lisiwasilishwe kwa ufasaha; lakini ikiwa linatoka moyoni, litapanda kwenda mahali Patakatifu ambapo Yesu anahudumu, na ataliwasilisha kwa Baba bila hata Neno moja la kuudhi, na lenye kigugumizi, bali kwa Maneno mazuri na yenye harufu nzuri ya ubani wa ukamilifu Wake mwenyewe
--------------------------------

Maswali: Taja majina ya mitume 12. Taja Heri nane. Soma kitabu cha Mlima wa Baraka kwa kuonja ladha nzuri ya zile Heri nane!

**SIKU YA 216.**
**(Agosti 3)**

# Mlima wa baraka-Sheria na kuishi maisha ya ukristo.

**Luka 6. Mathayo 5-7.**



Sehemu kubwa ya mafundisho ya mlima wa Baraka ilihusu sheria na jinsi ya kuishi maisha ya ukristo. Wengine walifikiri kwamba Yesu alikuja kutangua torati au manabii, akawaambia kwamba Neno la Mungu ni muhimu sana. Akasema mbingu na dunia zitapita ila Neno Lake hata tarakimu moja ndogo, halitaondoka kamwe. Mungu ameliweka Neno Lake juu zaidi, hata kwa Jina Lake. Hivyo mtu atakaye vunja amri Zake, ataitwa mdogo katika ufalme Wake. Wamezuka baadhi ya watu kusema Maandiko au sheria za Mungu si kitu bali cha muhimu ni kuwa na imani tu. Dini hii si ya Mwenyezi Mungu.

Maandiko au Neno la Mungu likiwa si kitu basi kila kitu kimekwisha, maana ni kwa Neno kila kitu kiliumbwa. Neno la Mungu ni tabia Yake. Neno linamwakilisha Yeye. Yesu aliwaambia watu alipokamatwa usiku ule wa Alhamisi, kwamba angeita malaika 10,000 wampiganie, ila hakuwaita "ili Maandiko yatimie"! Je umeona jinsi umuhimu Maandiko yalivyo? Kwamba japo alikuwa hatarini, na kifoni, alisonga mbele ili kulipa Neno utukufu wote unaostahili.

Basi mafarisayo walikuwa na tabia ya kusoma Maandiko, na kujifanya kuwa wanayajua sana ila hawakuyatendea kazi katika mitindo yao ya maisha. Yesu akawaagiza kuwa kila wanachofundisha mafarisayo wao wakifuate, ila wasiyafuate matendo ya mafarisayo, maana walikuwa wanafiki, hawakutenda yale walinena. Akawaambia kwamba "haki yao isipozidi ya mafarisayo hawataingia kamwe mbinguni." Akawafundisha furaha ya kweli inatokana na kumpokea Yesu na kutii amri Zake kwa kutenda mema na kwa kuwa wema ili Mungu atukuzwe. Yesu alipoishi duniani kulikuwa na Amri kumi, sheria za Warumi waliotawala, sheria za Musa, na sheria za marabi walizoongeza kutoka katika sheria za Musa.

Sheria za Musa zile za kutoa kafara zilikoma Yesu alipokufa, ila amri kumi ni sheria za kudumu kama kilivyo kiti cha enzi cha Mungu. Lazima tuwe waangalifu tunapoishi na watu wanafiki, na kufikiri kwamba tuna haki ya kutenda uovu kutokana na tabia zao. Ukiwa na ndugu au rafiki mnafiki, ni wakati wa wewe kusimama dede na kusema "Potelea mbali wengine ni wanafiki, ila mimi nitafanya mapenzi ya Mungu kwa neema Yake, ili niwape wengine mfano bora, na kufuta mifano mibaya ya waumini wanaoleta sifa mbaya kwenye kanisa."

Akaelezea kwa upana zile amri kumi, kwani mafarisayo walifikiri dhambi ni matendo tu, kumbe dhambi ni mawazo, nia na mwelekeo. Matendo huja baada ya mchakato huu. Yaweza hatujaua mtu kama amri ya sita inavyosema "usiue" ila tujue kuwa kila anayeona hasira au kumchukia mtu ameua. Akasema kama tumemkosea mtu, kabla ya kuleta sadaka twende kwanza na kuomba msamaha kwa huyu mtu, ndiyo tutoe sadaka ili Mungu apokee; maana hatuwezi kugusa mbingu bila kugusa watu. Mamilioni yetu ya pesa hayamshtui Mungu, Yeye ana shauku tujisalimishe Kwake, ili roho zetu ziokolewe.

Ni muhimu kupatana na mtu anayekushitaki mapema, la sivyo mambo yatakuharibikia. Akasema amri ya saba yasema usichukue mke au mume wa mtu (usizini), ila ukitamani kwamba yule mke au mume angekuwa wako, utakuwa ni sawa na yule aliyezini au kuchukua mke wa mtu tayari ila hakukamilisha tendo kutokana na kukosekana kwa nafasi. Hata katika wizi, tukitaka kuiba kitu fulani, na tusipate nafasi, inachukuliwa kama tumeiba tu. Mfano mtu akipanga kuiba baiskeli, akatoka darasani, na kukuta ile baiskeli imeondolewa, ni sawa na yule aliyeiba tu ile baiskeli, isipokuwa mazingira au nafasi haikumruhusu.

Baada ya kusoma Maandiko haya ya Yesu tunagundua hakuna asiye na dhambi! Hatuwezi kucheka wengine; itakuwa kama kumcheka mtu aliye kitandani kwenye wodi, ya wagonjwa waliozidiwa (ICU), kwa kuwa wewe upo kwenye wodi ya wagonjwa wa kawaida. Kwa kawaida mgonjwa mahututi anahitaji kuombewa ili apone, na huwa hatumcheki. Yesu alitaka tugundue jinsi dhambi ilivyo, na hitaji letu la Mwokozi kutusamehe na kutupa neema Yake. Akasema kama macho yetu ndiyo yanatukosesha kwa sababu tunatamani kwa njia ya kuona, basi ni bora macho yetu yangolewe, tuwe chongo na tungoje kurudishiwa mapya tukiingia mbinguni, kuliko kwenda jehanamu na macho yetu yote mawili na kisha tupotee. Na mkono au kiungo chetu chochote kikijaribu kutukosesha; bora kukikata kuliko kuingia motoni; maana mbinguni watu wote watapona vilema vyao, ila jehanamu hakuna kupona.

Akakataza kabisa mtu asimwache mke au mume wake, labda yule ambaye ameachwa na mwenzake mwovu ili aende kwa mwingine. Akawakataza kuapa kwa kitu chochote kwamba 'ndiyo' yao iwe 'ndiyo' na 'siyo' iwe 'siyo'. Watu wasiape "haki ya Mungu au mama yangu mzazi" bali ndiyo au siyo. Wengi hufikiri kuapa ni kitu cha kawaida kisicho na madhara, ila Neno la Mungu limetukataza. Twapaswa tulinde njia za moyo, vile tunavyoona, tunavyosikia, tunavyonusa, tunavyogusa n.k, ili tusitende dhambi.

Akawaambia wasilipe uovu kwa uovu, au wasitende sheria ya jino kwa jino au jicho kwa jicho. Akawaagiza mtu akiwapiga shavu la kushoto wageuze kulia, na anayetaka kuchukua koti wampe shati pia, na yule anayetaka waende naye maili moja waende mbili. Yesu alitaka watu wasilipize visasi, kamwe. Bali wapende maadui, maana hata watu wabaya wanawapenda ndugu zao ila wanawachukia maadui zao. Mungu Ndiye atafanya kazi ya kulipiza kisasi, maana anajua kipimo halisi cha rehema na haki kinachotakikana, bila kupitiliza kama sisi!

Walevi wana marafiki zao wananunuliana pombe, na hata majambazi huzawadiana nyara zao. Mkristo apaswa awe tofauti. Dini ya Kikristo haikubaliani na kuweka chuki, kuua mtu, kufanya hiana, au kupanga uovu kwa wengine. Dini ya Kikristo haituruhusu kufanya tunavyotaka kwa wengine au hata kwetu na kwa chochote kile ambacho Mungu aliumba! Kama binadamu ujifunze kusahau, na kusema "Dini yangu hainiruhusu kufanya ninavyopenda, bali kufanya vile Kristo anavyopenda yaani kujisalimisha kwake" au kufanya mapenzi ya Mungu.

Yesu mlimani alieleza kwa ndani umilele wa sheria aliposema ni za kudumu kuzidi nyota za mbinguni, anga, jua au ardhi tunayoikanyaga. Unaweza kuuliza Je Mungu hawezi kuchagua kuvunja sheria? Ndiyo! Mungu aweza kufanya atakavyo ila sheria zake ndiyo njia pekee ya afya, uzima na furaha. Kinyume cha sheria za Mungu ni uharibifu, machafuko na kifo. Sheria ya Mungu haiwezi kubadilika kwa vile inawakilisha au inatoa picha kamili ya utukufu Wake na tabia Yake ya Utakatifu na upendo.

Utakatifu unaonyweshwa katika sheria Zake, ndiyo maana sheria ina tabia ya kukataza usiue, usizini usiibe usi… usi…ili nasi tuonje tabia ya Mungu ya utakatifu na tabia Yake ya Upendo inaonyeshwa katika Injili, na Injili ni habari njema za ukombozi wa mwanadamu kupitia katika Yesu Kristo. Hata leo, tusifikiri kwamba hatuhitaji kutii sheria za Mungu, hii italeta uasi. Hata mbinguni hakuna anayevunja sheria za Mungu, na wala hutapenda kuwa karibu na mtu asiyejali sheria za Mungu. Zaburi yasema, wana furaha tele, wale waishikao amri ya BWANA. Ndiyo! Sheria za Mungu, na Maandiko ya Agano la Kale, bado zinafanya kazi kwa waumini wote. Na japo sheria za Musa za kuhusiana na kutoa kafara zilikwisha; bado tuna masomo fulani ya kujifunza toka katika sheria hizo, mojawapo ni kuonyesha kwamba sheria wakilishi zilizomwakilisha Yesu kama kivuli, alipokuja mwenyewe aliyekuwa akiwakilishwa, sheria hizo zikamaliza kazi yake, na ndiyo maana Yohana alisema,"Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya Ulimwengu" Sheria kama vile kuchinja kondoo kwa ajili ya kuondolewa dhambi zikakoma, bali amri kumi za Mungu ni za milele kwa vizazi vyote. Yesu ni Mwana-Kondoo wa

Mungu aliyechinjwa na Pasaka yetu, na kwamba sasa yupo hekalu la mbinguni kama Kuhani wetu Mkuu akituombea. Je! Huoni tulivyo na bahati, kwamba kila tunapofanya dhambi, hatuendi na familia zetu kununua kondoo ili tuchinje, bali yabidi tuwe na toba ya kweli, tuombe msamaha wa dhati.

Yesu alisema mtu atakayevunja Amri hata ndogo na kufundisha watu hivyo, basi ataitwa mdogo kabisa kwenye ufalme maana Mungu anataka furaha sasa kwetu na milele, hivyo anachukulia jambo hili kwa uzito na umakini sana. Anasema kwamba tukifundisha watu kinyume kwa sababu haiendani na furaha au ajenda zetu basi hatumwakilishi Yeye Mfalme Mkuu wa dunia. Hili ni jambo zito maana Yeye kila mahali anatuwakilisha vyema na kushughulikia maslahi yetu kwa upendo mwingi. Yesu aliposema hata adui tuwapende na wala tusiweke visasi, tumedhani kwamba hili haliwezekani. Ila Mungu anatupa tabia Yake ya kupenda adui. Yeye Ndiye aletaye mvua kwa wabaya na wema. Tunaokolewa kwa Damu ya Yesu, na neema Yake, ila sheria Yake moyoni ni matunda ya kumwanini, kumtegemea na kwa namna hiyo inakuwa ni sehemu ya tabia yako, haiwi mzigo, bali ni sehemu ya upendo Kwake Yeye aliye Mwokozi wa maisha yetu. Historia yatuonyesha kwamba wengi waliodai kumjua Mungu walikuwa wakatili na waovu. Yoyote anayeamini ile Kweli ila si mwaminifu, mpole na mvumilivu habariki wale waliomzunguka.

Kila mtu alielewa Yesu alipofundisha pale mlimani na siku zingine zilizofuata. Hata watoto nao, walitikisa vichwa vyao kuonyesha kukubaliana, walipomsikiliza Yesu wakiwa na wenzao. Mafundisho Yake hayakuwa magumu. Mfano kama hakuna aliyetaka kupigwa, Kwa nini apige wengine? Kama hakuna aliyetaka mwingine amvunjie penseli yake, mwanasesere (toy) au gari lake, basi asimfanyie mwingine uovu ule. Yesu aliweka sheria rahisi, ili kutusaidia kuishi kwa amani, utulivu na maelewano. Mafundisho Yake yalikuwa ya peke yake, na kama kila mtu angeyatenda, basi kila mtu angeishi kwa amani. Hatupaswi kungoja wengine waanze kutenda Yesu aliyoagiza kabla yetu, La! Yeye alisema tutendapo yale ametuagiza tutaishi maisha ya furaha, manufaa na baraka, hata wengine wakiwa wanafanya kinyume. Kwa maneno mengine, haijalishi kile mwingine anafanya kwetu, sisi tutende Maagizo ya Mungu, Naye atashugulikia dhuluma zinazotokea.

Yesu alitambulika kutumia usiku kucha katika maombi, kama alivyofanya katika usiku ule kabla ya kuchagua timu ya mitume 12 ambao siku moja wangeipeleka injili duniani (Luka 6:12, 13). Mfalme wa mbinguni, wakati akiwa katika huduma Yake duniani, aliomba sana kwa Baba Yake. Alisujudu mara nyingi kwa maombi usiku kucha. Roho Yake mara nyingi ilikuwa na huzuni kadiri alipohisi nguvu za giza za dunia hii, na akaondoka katika mji ulio na shughuli nyingi na makelele, ili kutafuta sehemu iliyojitenga ili kufanya maombi Yake. Mlima wa Mizeituni ulikuwa ni sehemu pendwa ya kimbilio kwa Mwana wa Mungu kwa ajili ya maombi Yake. Mara nyingi baada ya umati kuachana Naye kwa ajili ya pumziko la usiku, hakupumzika, japo alikuwa amechoka kwa kazi ya siku nzima… Wakati mji ukiwa umetulia tuli! Na mitume wakiwa wamerudi majumbani mwao ili kupata burudiko la usingizi, Yesu hakulala. Maombi Yake yalikuwa yakipanda kwa Baba Yake kutoka katika Mlima wa Mizeituni kwamba mitume Wake na sisi tulindwe dhidi ya mivuto ya uovu ambayo tutakutana nayo kila siku duniani, na kwamba nafsi

Yake iweze kuimarishwa na kuandaliwa kwa ajili ya majukumu na majaribu ya siku inayofuata. Usiku kucha, wakati wafuasi Wake wakiwa wamelala, Mwalimu wao alikuwa akiomba … Kielelezo Chake hicho kimeachwa kwa ajili ya wafuasi Wake!

*Unapotaka kuzungumza kwa jazba au hasira, funga mdomo wako. Usitamke neno lolote. Omba kabla ya kuzungumza, na malaika wa mbinguni watakuja kukusaidia na watawarudisha nyuma malaika wabaya, ambao wangekuongoza kumvunjia MUNGU heshima, kuiletea aibu au fedheha kazi Yake Mungu, na kudhoofisha roho yako mwenyewe.

------------------------

Maswali: Orodhesha majina ya mitume 12. Kumchukia mtu au kumtamani mke wa mtu, ni sawa na kuvunja amri zipi? Kwa nini Yesu alisali usiku mzima? Kwa nini tusilipize kisasi "jino kwa jino au jicho kwa jicho"? Kwa nini ni dhambi kulipiza kisasi? Kwa nini ni muhimu kuomba msamaha tukimkosea mtu? Je unajua popote Mungu aliposema, amri moja kati ya zile kumi hatupaswi kufuata? Kwa nini Sheria na Maandiko ya Mungu ni ya kudumu? Kwanini ni kosa kubwa kutozitii zile Amri Kumi? Je! Ni amri gani wewe unaona kabisa huitii, kati ya zile kumi? Je! Unapata kufanya nini katika kutii hiyo?

**SIKU YA 217.**
**(Agosti 4)**

# Wana Heri au Wana furaha, au Wamebarikiwa.

**Mathayo 5**



Yesu hakuwa mponyaji tu, bali alikuwa Mwalimu mkuu wa wote. Alipowasaidia watu alizungumza kwa njia rahisi na wazi, na watu wakafurahi na kupenda kumsikia. Alitoka mbinguni kutuambia upendo wa Mungu. Twapasa kuwa watoto Wake wenye mioyo safi, tunaosema Kweli na wenye kutii. Hakubagua mtu, maana alimchukulia kila mtu ni raia mtarajiwa wa ufalme wa mbinguni. Mungu hana upendeleo. Ukiangalia hizi heri, zinakuwa kama zina walakini, au zinasema kinyume cha mambo ambayo yanaeleweka na watu wote. Mfano wana furaha walio na umasikini wa moyo maana ufalme wa mbinguni ni wao. Mara nyingi kama vile kitabu cha Ayubu kilivyosema, watu walifikiri mtu akimtegemea Mungu hatakuwa na huzuni bali mali na vicheko kila mara. Hii si kweli, kwani Ayubu na wengine waliomcha Mungu waliwahi kuwa na huzuni ya moyo.

Kuwa na umaskini wa kiroho ni kuwa mnyenyekevu na kujiona ni mhitaji wa haki ya Kristo na si haki yako mwenyewe. Wale ambao jumuiya inawakataa au kuwakana kwa kuwa ni maskini, watoza ushuru au malaya hujiona hawana kitu

cha kuwasilisha ila neema ya Mungu tu iwasaidiayo na kuwafunika. Wanamlilia Mungu awape rehema, na hii inawabidisha kutubu na kuona huzuni kwa makosa yao. Jambo lililo jema kwao si tu urithi wa ufalme wa Mungu bali pia wanafarijiwa na Mungu Mwenyewe kwa kupewa msamaha na hakika ya wokovu wao. Tukipewa rehema inakuwa rahisi hata sisi kurehemu watu wengine kwani tunajua tumebebwa na Mwenyezi Mungu.

Yesu akatoa mfano wa farisayo aliyekwenda hekaluni. Huyu alijipima na kujiona ni mwenye haki, akidharau wengine wote. Yesu alionyesha kwamba dhambi inaweza kumfuata mtu hata kanisani, kwa sababu inakuwa imo mawazoni kwanza. Dhambi hii ni kiburi cha mambo ya kiroho. Yule Mfarisayo alifika hekaluni na kumwona mtoza ushuru, nao wote wawili waliendelea na sala.

Yule Mfarisayo alisimama akiomba moyoni mwake kwa kutaka kujionyesha kwa watu na wala si kuzungumza na Mungu, kwa maneno mengine alikuwa akiwasengenya watu wengine kwa Mungu akisema "Eh Mungu nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, majambazi, wadhalimu, wazinzi, wala si kama huyu mtoza ushuru. Nafunga mara mbili kwa juma; hutoa zaka katika mapato yangu yote. Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipiga piga kifua kwa kujinyenyekeza na huzuni akisema "Ee Mungu unisamehe na kunirehemu, maana najua mimi ni mwenye dhambi."
Yesu akauliza ni nani aliyerudi nyumbani kwake amehesabiwa haki? Wakajibu ni yule aliyejidhili. Basi Yesu aliwaambia ajikwezaye atadhiliwa au kushushwa na ajidhiliye atakwezwa. Tunapoomba tuombe kwa Mungu, na si kwenda kumfahamisha Mungu uzuri wetu au kuleta umbeya wa watu. Mungu ndiyo aonaye uzuri wetu, na atatupa thawabu. Mungu hakusema heri wale wenye akili nyingi darasani, wazuri wa uso, wenye pesa, wenye meno mazuri, au mafundisho sahihi ya imani; bali alisema heri wenye moyo safi. Mafundisho ya Mlima wa baraka yanataka tusiwe wabinafsi.
Moyo na nia, zapaswa kuwa safi, yaani mawazo yakiwa safi, hata maneno na matendo yatafuata usafi. Kuelewa mafundisho ya ile kweli sahihi ni muhimu, ila moyo sahihi ni kioo cha imani ya mtu ya kila siku. Kuwa mshiriki wa kanisa fulani ni tofauti na kuwa mkristo au mtu wa Mungu. Kwanza tunapaswa kuwa watu tunaomwamini Mwenyezi Mungu, kisha dhehebu letu!

Jifunze heri moja moja, mfano; kuwa mpatanishi ukiona wenzako wanapigana, wanakosana, wanalumbana au kugombana, chukua nafasi kuwa mpatanishi na si mchonganishi. Wewe ni chombo cha Mungu kupatanisha watu, pale penye chuki ulete upendo, penye majeraha ulete uponyaji na penye giza ulete mwanga na matumani, pale penye huzuni ulete furaha. Usingoje watoto wengine wakupende, wakufariji au kukusamehe wewe, bali wewe uwe wa kwanza kupenda watu, kuwafariji na kuwasamehe. Kuishi maisha ya utakatifu utakapokuwa mbinguni ni rahisi sana, ila kuishi maisha ya utakatifu duniani ni mtihani mwingine ambao tunapaswa kuushinda sasa.

Usiwe mchochezi au mtu anayependa kugombana na wengine. Maisha ya mtu yana milima, mipando na kona kona nyingi, na hata mateso, na hasa kama mtu huyo anamjua BWANA. Yesu, na mitume waliishi kwa dhiki. Kumwamini Mwenyezi

Mungu kumeleta kuchukiwa na kuteswa, toka wakati wa Habili aliyeteswa na kuuwawa na kaka yake Kaini.
Ukimwamini Mungu umetangaza vita hata kwa jamaa zako wa karibu. Mfalme Nero wa Rumi aliwachoma moto waumini. Wakristo wengine walishonwa kwenye ngozi za kondoo na kutupiwa mbwa mwitu wakararuriliwa vipande vipande. Hata Yesu hakuepuka mateso, hadi akatundikwa msalabani. Mateso yatajirudia tena mwisho wa dunia. Mateso haya yatakayowahusu watu wa Mungu, tunayasoma katika Ufunuo 13.

Mateso yataendelea kwa wote wanaotafuta haki ili kuwachuja na kuwafanya wawe na tabia ya Mungu. Tabia ya Mungu inafananishwa na kito cha thamani chenye kung'ara. Hii ni tabia ya kutojifikiria mwenyewe na ya kuhudumia wengine. Kumbuka mateso ya kujitakia hayana faida, ila yale ya kuteswa kwa ajili ya haki. Hekima ya Mungu ni ya ajabu, na haina makosa wakati wote kwa wale wanaoamua kuifuata

Basi wote wanaoamua kumfuata Mungu lazima wamwamini kikamilifu, wamshuhudie, na kumhudumia. Leo, Mahubiri ya Mlimani yanachukuliwa kuwa kama Maneno na nzuri zaidi ya Ukristo, lakini ni vigumu sana kutekelezwa . Twapaswa kuwa chumvi, twapaswa kuwa nuru leo hii. Soma Mathayo 5 tena na ufikirie jinsi unavyoweza kuishi Mahubiri haya maishani mwako leo.

*MUNGU angefanya kazi kwa nguvu za kushangaza kwa watu Wake leo ikiwa wangejiweka chini ya uongozi Wake kikamilifu. Wanahitaji kufungamana na Roho Mtakatifu kila wakati. Ikiwa kungekuwa na maombi zaidi katika mabaraza ya wale waliobeba majukumu, unyenyekezaji wa moyo zaidi mbele za MUNGU, tungeliona ushahidi mwingi wa uongozi wa Bwana, na kazi yetu ingelisonga mbele haraka.
------------------------

Maswali: Je Mfarisayo alisali akitumia maneno gani? Je Mtoza ushuru alisema maneno gani kwenye sala yake? Kwa nini Mateso huja kwa wacha Mungu? Kwa nini kujipenda wenyewe kuliko Mungu ndicho kiini cha dhambi zote? Kwa nini kujisalimisha kwa Mungu ni muhimu? Tunaelekea kufunga historia ya dunia kulingana na unabii, Je hii inahusikaje na mateso? Je, chakula bila chumvi kinakuwaje? Je, chumba bila mwangaza kinakuwaje? Tunawezaje kuwa na moyo safi, Soma 1 Yohana 1:9!

**SIKU YA 218.**
**(Agosti 5)**

# Sala ya BWANA aliyotufundisha tuombe.

**Mathayo 6**



Yesu akawaambia wanafunzi Wake wawapende jirani na adui zao pia. Wawaombee wale wanaowaudhi, maana Baba wa mbinguni huwaangazia jua Lake wema na waovu pia. Mungu huwapenda hata wasiopendeka; maana Biblia inasema, tukiwapenda wale tu wanaotupenda, hatutakuwa tumefanya kitu tofauti, maana hata watu wabaya hupenda ndugu zao na marafiki zao tu. Akawaambia "muwe wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu." Ukamilifu huu ni kukomaa kwa mambo ya kiroho kwa kujisalimisha kwa Yesu ili atubadili mawazo, nia, na kisha tabia, ili tufanane na Kristo.

Akasema msifanye mema ili watu wawatazame na kuwasifu, maana kinachojalisha ni jinsi Baba wa mbinguni anavyoona na siyo watu. Siku zile wengi walitoa sadaka kwa kujionyesha, wakatoa kwa uwazi, ili kila mtu aone walichotoa. Wakifanya hivyo Yesu anasema watakuwa "wamekwisha kupata thawabu yao", yaani watu wameshawasifu tayari na kuwashabikia. Yesu anaelekeza tunapotoa sadaka au kumsaidia mtu kwa jambo fulani mkono wetu wa kushoto usijue ufanyalo mkono wa kuume. Sadaka ni kitu cha siri, ambacho ni Mungu tu Ndiye anapaswa ajue. Kama tukitoa sadaka kwa kufuata utaratibu huo ndipo tutakapopata baraka. Tukiwa

na sadaka, tusiingie kuabudu bila kuileta, maana baraka zimeahidiwa, na kama hatuna, Mungu anajua kwamba kuleta mioyo yetu Kwake ndiyo kipaumbele ya yote.

Kisha Yesu akaagiza, tunaposali, tusisali kusudi watu watuone, na wala tusisali sala ndefu, tukipayuka payuka. Alisema tunaposali tufunge milango, na kuomba sirini na "Baba yetu wa mbinguni aonaye atatujazi." Yesu alitumia muda mwingi kusali, ndipo wanafunzi walienda kumwomba Yesu awafundishe kusali. Wengi hata leo wauliza nisali namna gani? Je unajua kusali? Je mtu anazungumzaje na Mungu? Je maneno yanakuishia unapozungumza na Mungu bali ukiwa na marafiki muda hautoshi na unajisikia una kikapu cha maneno? Je inatubidi tutamke maneno fulani, ya kupayuka, na kukariri kama tunavyofanya kwenye mchezo wa kuigiza? Je! Tunamwitaje Mungu tukianza kusali? Pengine una marafiki ambao hawajawahi kusali, na hawajui waanzaje kuzungumza na Mungu. Hawa waweza kuwafundisha kusali.

Mungu anasema tuzungumze Naye kama Baba yetu, anayetupenda na kutaka tuwe na mahusiano Naye. Anataka tumwambie furaha na huzuni zetu. Yesu alizungumza na Baba wa Mbinguni daima. Mara zingine aliomba usiku kucha akipenda kuwa karibu na Babaye na kuomba uongozi wa kazi Yake duniani. Wanafunzi Wake walimwambia Yohana mbatizaji aliwafundisha wanafunzi Wake kuomba, naye pia angewafundisha. Kuomba ni kuzungumza na Mungu kama rafiki yetu, hatuhitaji kuwaonyesha watu tukiomba. "Nenda chumbani uombe, zungumza Naye kama unavyozungumza na rafiki." Hatuna haja ya kusema mengi sana, maana Mungu anajua yote yaliyoko moyoni. Mwambie furaha zako, na huzuni zako. Yesu aliwapa mfano au namna iwapasayo wanafunzi Wake kusali, ambayo inaitwa Sala ya BWANA. Kuomba kunaondoa wasi wasi au huzuni, kwani tukiomba tunamwachia Mungu shida zetu zote maana Yeye ana uwezo na mamlaka yote ya kuzitatua.

Sala ya BWANA ni vyema kila mtoto au mtu aijue na kuikariri. Mungu anajua tunayohitaji, si lazima kusali sala ndefu, hasa tunapokuwa mbele za watu. Haitupasi kurudia rudia bila kutafakari wakati tunapoomba. Tukisali tuseme hivi: "Baba yetu uliye mbinguni, Jina Lako litukuzwe, Ufalme Wako uje Mapenzi Yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni Wako, na nguvu na utukufu, hata milele. Amina."

Kwa sala hii tunagundua kwamba twapaswa kujua Mungu ni Baba yetu anayetupenda. Yeye ni Nafsi hai halisi na muhimu kwa maisha yetu ya kila siku na milele. Twapaswa kumwomba atufundishe kuitii sauti Yake na kujisalimisha Kwake, ili tuweze kuwa raia wa ufalme wake siku moja. Ni Yeye Ndiye anayetupa mahitaji yetu yote, iwe chakula, mavazi au malazi. Twahitaji kusamehewa dhambi zetu na kusamehe wengine, kila siku. Twapasa kumwomba Mungu atusaidie tusifanye dhambi, au kujaribiwa kuelekea njia ile pana yenye uovu. Ufunguo wa maisha ya kiroho ni kujisalimisha au kujitoa Kwake. Na kujiepusha na nadharia nyingi za uongo zinazokuja kuhusu Maandiko Matakatifu, Uungu au Miujiza.

Tunasamehewa makosa yetu tu, pale tunaposamehe wengine. Tusiposamehe nasi hatusamehewi. Tujifunze kutoweka kinyongo au kulipiza kisasi. Na pale tunapofunga tusiwe wanafiki tukikunja nyuso ili watu watuone. Tukifunga tupake mafuta ili ngozi isikunjamane na Baba yetu wa mbinguni aonaye sirini mfungo wetu atatujazi. Si kwamba Baba yetu hajui mahitaji yetu, ila tukimwambia mapenzi yetu, haja au uchaguzi wetu, tunampa mamlaka au uhuru aendelee mbele, na kutufanyia kwa mamlaka na uwezo Wake wote, akijua tumempa 'ruksa' atutendee yale tumemwomba na si kwamba anatulazimisha.

Yesu ameahidi kusikiliza maombi yetu, na ndiyo maana akatufundisha kuomba. Sala hii imegawanyika katika mambo haya; kumsifu Mungu na kumshukuru, kuomba mahitaji yetu, kuomba msamaha na kusamehe. Twapaswa kuomba kila siku, kwani inatusaidia kujua njia za Mungu, na kumweleza Mungu yale mambo ya kila siku yanayotuhusu katika kujenga mahusiano na watu na Mungu. Tusijiombee mahitaji yetu tu bali tukumbuke na wengine pia. Tusisahau Mungu anapenda kutupa kila hitaji letu, na kuna mengine hawezi kutupa endapo hatutaomba. Kwa kuomba, tunampa Mungu, mamlaka na uchaguzi wetu wote kutufanyia mambo fulani.

Tusijiwekee hazina duniani kwa kutaka tuwe na vitu vingi au utajiri. Kuwa na vitu vingi na vizuri isiwe ndiyo kitu muhimu kwetu, bali mahusiano Naye. Tuweke hazina zetu mbinguni ambapo nondo, wezi au kutu hawatazitaharibu hivyo zitadumu. Kuweka hazina mbinguni ni kusaidia wenye mahitaji na kusaidia kazi ya BWANA ili wengi wapate injili. Mahali hazina yetu ipo, ndipo mioyo yetu itakuwepo. Yaani tukipenda pesa, basi mioyo yetu itakuwa kwenye pesa na ndoto za pesa, na tukimpenda Mungu na kazi Yake au watu, basi mioyo yetu itakuwa imekita kwenye hazina za mbinguni, na siku moja tutafika huko.

Yesu akiwaona wengi wana mashaka, mifadhaiko, na wasiwasi kwa ajili ya matatizo mengi aliwafundisha kuwa hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili, Shetani na Mungu. Lazima atampenda mmoja kuliko mwingine. Kuna mabwana wawili tu, na falme zao ni kinyume cha nyingine. Kisha Yesu akatoka kwenye mawazo na matendo na kwenda kwenye vitu. Akitaka kuwakumbusha kwamba vitu vinaweza kuwa Mungu. Akasema tusisumbukie maisha mno, kwamba tule nini au tuvae nini, maana watu waovu au makafiri wanasumbuka sana na vitu hivyo. Ila sisi tutafute ufalme wa Mungu na haki Yake yote, kisha hayo mambo mema tutazidishiwa.

Ndege wa angani hawatoi jasho kulima, ila Mungu huwalisha. Nasi binadamu tu bora zaidi ya ndege, maana tuliumbwa kwa mfano wa Mungu na Yesu alikuja kufa kwa ajili yetu na si kwa ajili ya ndege au mimea. Hata tukisumbuka sana hatuwezi kuongeza urefu wetu. Akisonda maua, akasema wafikirie maua ya mashambani hayatoi jasho au kufanya kazi yameapo; ila hata mfalme Sulemani katika fahari yake hakuvikwa kwa uzuri kama maua. Mungu huyapa maua uzuri wa ajabu, japo yananyauka keshoye, basi sisi binadamu je, hatatuvikwa vizuri zaidi "enyi wenye imani haba." Yesu akasema "tusisumbuke na ya kesho, au kuwa na hofu na mahangaiko, kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe, yatosha siku moja maovu yake."

Mungu anajua fika kila tunachohitaji, sisi tumwamini tu! Yeyote anayemwamini humpa amani inayopita akili, hata kama wengine wanahaha, wakihangaika na mifadhaiko hapa na pale sisi tutakuwa shwari. Si kwa vile hakuna shida, bali Yesu ametuliza dhoruba zote za moyoni mwetu, na kuchukua mazito ya matatizo yetu na kuyafanya kuwa mepesi. Utauwa na kuridhika ni faida kubwa, tuishi kwa mambo ya siku moja tu, japo kila mmoja amepangiwa siku zake za kuishi, lakini ni vema uzito mkubwa akauweka katika siku aliyojaliwa kuiona, maana kesho hatuiui kama tutaifikia. Hii haina maana kwamba tusiweke mipango, mikakati au malengo yetu ya muda mrefu la hasha, haina maana hiyo.

*Maombi Yataleta Uwezo wa Kushinda- Lazima tuwe na silaha zote za MUNGU na tuwe tayari wakati wowote kwa vita dhidi ya nguvu za giza. Wakati majaribu na mitihani vinatukimbilia kwa kasi, twendeni kwa MUNGU na kuteseka na kuhuzunika Naye katika maombi. Hatatürudisha na mikono mitupu , lakini atatupa neema na nguvu za kushinda, na kuvunja nguvu za adui.

----------------------------

Maswali: Kwa nini tusisumbukie maisha kama watu wa dunia? Kwa nini mtu hawezi kutumikia mabwana wawili? Kusali maana yake ni nini? Mara ngapi kwa siku twapaswa kusali? Tunawezaje kujiwekea hazina mbinguni? Kwa nini tutoe sadaka kwa siri? Kwa nini inahitajika imani kuweka hazina zetu hata kwenye benki ya duniani? Kwa nini si vizuri kupenda pesa? Unafikiri Kwa nini Sala ya BWANA haisemi Baba yangu bali Baba yetu? Kariri sala ya BWANA.

**SIKU YA 219.**
**(Agosti 6)**

# Ombeni nanyi mtapewa, Bisheni nanyi mtafunguliwa, tafuteni nanyi mtapata.

**Luka 11 na Mathayo 7.**



Yesu akaendelea kusema tusihukumu watu maana kwa kuhukumu watu nasi pia tutakuhukumiwa kipimo kile kile tupimacho. Kama binadamu hatujui Kwa nini mtu amefanya lile alilofanya, au kilicho ndani ya moyo wake, hivyo twapasa kumwombea mtu huyo ili abadilishwe na Kristo Mwenyewe. Maisha ya mkristo yahusu mahusiano yake na Mungu na pia binadamu wenzake. Tuanze kutoa kibanzi kilicho kwenye jicho letu, ndipo tunaweza kuwa msaada wa kutoa boriti kwenye macho ya wenzetu. Tusiwe wanafiki kwa kuona wengine wafanya baya hili au lile, wakati sisi tunafanya maovu makubwa zaidi yao. Kibanzi ni kama kuwa na punje ya mchanga kwenye macho, na boriti ni kama kuwa na penseli kubwa kwenye jicho.

Tuombe hekima pale tunapopaswa kukaripia na kukemea au pale ambapo, Jina la Mungu linapotukanwa au watu wasio na hatia wanapoumizwa. Kujaribiwa si udhuru wa kutufanya tufanye dhambi. Tusitupe Lulu au vitu vya thamani kwa nguruwe, ambao ni mfano wa watu ambao hawaoni thamani ya hazina za mambo yao ya kiroho. Yesu akatoa mfano wa mtu aliyepata wageni usiku wa manane, na kwenda kubisha kwa rafiki yake amkopeshe mikate mitatu maana rafiki yake aliyetoka safari, amefika akiwa na njaa na hana chochote cha kumpa. Yule mwenye nyumba kwa uvivu na usingizi akasema "usinitaabishe; mlango umekwisha fungwa, nasi tumelala kitandani, mimi na watoto wangu, siwezi kuondoka nikupe."

Yule mtu japo hataondoka kitandani mwake kutoa ule mkate kwa uvivu na usingizi alionao, atajikokota tu na kuamka na kumpa chakula, hata kama anakuwa amenuna, si kwa vile ni rafiki yake tu, bali kwa vile anavyomng'anga'niza asipange kutoka pale mlangoni. Maana jinsi huyu mtu anavyozidi kumwomba na kulalama, hataweza kupata usingizi, hivyo ataamka na kumpa ili aondoe udhia, na kisha arudi kwenye

usingizi wake. Yesu akasema kama mtu wa dunia tu asiye na upendo kama Mungu, bali kwa kubugudhiwa aweza kuamka na kumsaidia jirani yake hitaji lake, Je Yeye Mungu, si atafanya zaidi? Mfano umetolewa kwa kutofautisha, na si kulinganisha tabia ya Mungu. Mifano haitoi picha ya kila kitu, hivyo unamega kile kipande cha fundisho lake, na kuacha mengine!

Yesu akasema "ombeni nanyi mtapewa, tafuteni mtaona, na bisheni mlango nanyi mtafunguliwa." Kila mtu atakayeomba atapata, kila mtu atakayebisha mlango atafunguliwa na kila mtu atakayetafuta atapata. Maana Mungu ni zaidi ya wazazi; zungumza Naye kama rafiki na mzazi mkuu kwa maombi. Mtumaini Yeye maana anakupenda sana. Hakuna mzazi atakayempa mtoto wake jiwe akimwomba mkate, au ampe nyoka akimwomba samaki, au ampe ng'e akimwomba yai. Basi endapo binadamu waovu wanajua kuwapa watoto wao vipawa vyema, je Baba wa mbinguni ataachaje kutujali sisi zaidi ya wazazi wetu wa duniani?

Baba yetu wa mbinguni Yupo tayari kutupa kipawa cha Roho Mtakatifu sote tumwombao. Yesu alisema hivi akimaanisha tutapewa yote tunayoomba yaani yale yasiyotukwaza kujenga tabia ya kuishi milele. Yesu akakazia zaidi kuhusu Roho Mtakatifu atakavyopewa kwetu kila tumuombapo ili atusaidie kwa mambo mengi kama kutukumbusha la kufanya, kutusaidia kuomba, kutufariji, kutukanya tunapokosea, kutushauri maamuzi magumu, kutupa nguvu na kutusaidia kuwaambia wengine kuhusu habari njema za ufalme. Mengine mengi tukiomba tunapewa papo hapo kama msamaha wa dhambi, Roho Mtakatifu, kupenda na kujali wengine, kuwa na roho ya kuhudumia, au neema ya Mungu.

Roho Mtakatifu humwagwa kwa watoto Wake wote wamwaminiao. Roho Mtakatifu ni Mungu, ni nafsi ya pili ya Uungu, kama vile tunavyomjua Mungu Baba na Roho Mtakatifu (Utatu Mtakatifu). Jina jingine la Roho Mtakatifu ni Roho wa Mungu, na Mfariji. Roho Mtakatifu ni zawadi au karama kwa kila mtu, mtoto au mtu mzima. Yesu aliwaahidi mitume wake pia kabla ya kuondoka, atawapa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni wa Muhimu sana, na ana tabia kama ya Yesu, yaani rafiki na mwenzi wetu.

Yesu akaendelea kusema tuwatendee watu mema, maana ndiyo kutimiza Maandiko yote, iwe torati au manabii. Kuna njia mbili tu, moja yenye mlango mwembamba na nyingine ina mlango mpana. Njia pana yenye kuonekana na lami na marembo mazuri hiyo yaingia upotevuni, ila ile nyembamba ya vumbi na isiyopendeza inaenda uzimani. Yesu akakumbusha tena "Jihadharini na manabii wa uongo" hawa wanakuja kama watu wema wamevaa mavazi ya kondoo ila ndani ni mbwa mwitu wakali. Hawa waweza kurarua na kuumiza watoto wa Mungu. Akasema mti mwema huzaa matunda mazuri na mti mbaya au mwovu huzaa matunda mabaya. Twapasa kujua jinsi ya kupima manabii wa Uongo na wale wa kweli.

Haitupasi kuhukumu watu, bali tutawatambua watu kwa matunda mema au mbaya. Matunda mema ni kama upendo, amani, furaha, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, kiasi, na upole. Matunda mabaya au ya mwili ni mengi kama vile uchawi, uadui, fitina, hasira, uzushi, uasherati, husuda, uchafu, ibada ya sanamu,

ulevi, ugomvi, na mambo yanayofanana na hayo. Mtu atakayeingia mbinguni ni yule afanyaye mapenzi ya Mungu wa mbinguni, yaani mwenye matunda mazuri. Siku ya mwisho wengi watadai wamefanya unabii kwa jina la BWANA au miujiza wakisema “tumetoa pepo kwa Jina Lako na kufanya miujiza mingi.” Ndipo BWANA atasema “sikuwajua ninyi kamwe ondokeni Kwangu watenda maovu.” Ndipo kutakuwa na kilio na kusaga meno.

Kila mtu atakayesikia Maneno ya Mungu atafananishwa na mtu mwenye akili aliyejenga nyumba yake kwenye mwamba. Mvua ikanyesha, pepo zikavuma na kuipiga nyumba, nayo haikuanguka, kwa vile msingi wake uligota kwenye mwamba. Mtu asiposikia Maneno ya Mungu, atafananishwa na mjinga ambaye alijenga nyumba kwenye mchanga, na mvua, mafuriko na pepo zilipovuma na ziliizoa ile nyumba ikaanguka puu kwa kishindo kikubwa. Hata hivi leo sisi tujenge nyumba au imani na matumaini kwenye Mwamba ambaye ndiyo Kristo.

Yesu mlimani pia alitahadharisha kwamba jinsi tunavyoishi maisha yetu ndivyo italeta tofauti. Maana wengi watasema mbona tumetoa unabii kwa Jina Lako au kutoa pepo au kufanya maajabu. Atasema siwajui, maana hawakumruhusu awasaidie kuishi kwa kanuni Zake, bali walitaka kuishi wapendavyo. Yesu alimaliza kuzungumza haya kwenye mlima wa baraka, na makutano walishangaa mno kwa mafundisho Yake; kwa vile aliwafundisha kama mtu mweye amri na mamlaka, na si kama waandishi na mafarisayo. Hata yale aliyofanya yalikuwa ni ya mamlaka, kwani hakuna binadamu aliweza kuyafanya. Sauti Yake ilisikika kwa wote bila kipaza sauti, na kila aliyesikia aliona ujumbe ule unamfaa yeye. Kisha akashuka mlimani na wanafunzi wakamfuata.

Hapa ndipo Yesu alipomaliza kuzunguma mambo ya Yohana mbatizaji kama mtengeneza njia na alikuja kuwapa watu ujumbe ila hawakusikia. Kwa vile walifanana na watoto sokoni walioitana na kusema “Tuliwapigia filimbi wala hamkucheza, tuliomboleza wala hamkulia.” Maana Yohana mbatizaji alivyokuja hakunywa divai wala mkate watu walisema ana pepo. Yesu alikuja anakula na kunywa, watu wakasema ni mlafi huyu, rafiki wa watoza ushuru na wenye dhambi. Watu hawa ilikuwa vigumu kuwapendeza, walikuwa wakikosoa kila mtu wa Mungu wakifikiri wao wanatenda mema.
Twapasa kujenga maisha yetu kwenye kanuni za Yesu na si ubinafsi au nadharia za kibinadamu.

*Omba kwa imani. Na hakikisha unauleta mtindo wako wa maisha upatane na maombi yako, ili upate baraka ambazo unaziombea. Hebu imani yako isidhoofike, kwani baraka zinazopatikana zinalingana na imani inayotumika. “na iwe kwako kulingana na imani yako”. Na mkiwa na imani, chochote mtakachoomba katika sala, mtapata.” Mathayo 9:29; Mathayo 21:22. Omba, amini, furahi. Mwimbieni MUNGU sifa kwa sababu amejibu maombi yenu. Mchukue kwa Neno Lake. “Yeye ni mwaminifu aliyeahidi.” Waebrania 10:23. Hakuna ombi hata moja la dhati litakalopotea. Mfereji upo wazi; kijito kinatiririka. Kinabeba pamoja nacho sifa za uponyaji, kinamimina umeme wa uzima, afya na wokovu.

*MUNGU Anatamani Kutufanyia Mambo Makubwa — Kazi yetu ni kuomba na kuamini. Kesheni mkiomba. Kesha, na ushirikiane na MUNGU anayesikia maombi. Iweke akilini mwako kwamba “sisi ni watenda kazi pamoja na MUNGU.” 1 Wakorintho 3: 9. Sema na tenda kwa kupatana na maombi yako. Itafanya tofauti ya milele kwako endapo jaribu litathibitisha imani yako kuwa ya kweli, au kuonyesha kwamba maombi yako ni mfumo fulani tu.


--------------------------

Maswali: Kwa nini tusihukumu watu? ‘Tusitupe Lulu au vitu vya thamani kwa nguruwe’ ina maana gani? Vitu gani kwa mawazo yako ukiomba utapewa na vipi hutapewa?  Mtu aliyejenga nyumba yake kwenye mchanga anafananishwaje? Kwa nini mtu aliyelala aliamka kumpa jirani yake mkate? Roho Mtakatifu ni Nani? Roho Mtakatifu ana kazi gani? Taja mambo mane yanayokujulisha kama mtu ni nabii wa uongo?

**SIKU YA 220.**
**(Agosti 7)**

# Mtumishi wa akida wa Kirumi aponywa.

**Luka 7**



Alipokwisha kumaliza Maneno kwenye mlima wa baraka aliingia Kapernamu na pale mtumwa wa akida mmoja wa Kirumi, alikuwa mgonjwa akikaribia kufa; naye aliposikia habari za Yesu alituma wazee wa Wayahudi kumwomba aje kumponya mtumwa wake. Akida huyu alipenda watu, hata watumwa wake. Alikuwa ameondoa ubaguzi wa Warumi, na chuki waliyokuwa nayo kwa watu wa-mataifa mengine waliyoyateka. Wazee wale wakamwambia Yesu kwamba huyu akida japo ni Mrumi, anastahili umsaidie kwani analipenda taifa letu na alitujengea sinagogi. Alishugulikia jamii yao na kuona maslahi yao yanatimizwa. Wazee hawa walifanya jambo zuri, maana zamani zile Wayahudi walitazamia Masihi akija kutakuwa na karamu kubwa ambayo Wayahudi tu ndiyo watakaribishwa na watu wa mataifa hawatakuwa sehemu ya mema yoyote.

Japo mtumwa alikuwa ana thamani ndogo hata kuliko vitu, akida huyu aliwapenda watu, na hakuwa mkatili kwa watenda kazi wake. Yesu alijaribu kufikia watu wote, wenye madaraka, maskini, warefu, wafupi, wageni, wenyeji, wanawake, watoto na wanaume. Utajiri wa mtu haukumpa hofu. Kipaumbele Chake daima ni roho za watu ziokolewe. Hata leo pia tusiogope kuwaambia wale wa kwenye ngazi za juu au mamlaka, watoto wa matajiri, mawaziri, maraisi, wafalme, wafanya biashara, na wakuu wa majeshi. Wote hawa wanahitaji kusikia habari njema. Mara nyingi watu kama hawa wanatengwa maana watu wanaogopa kuwafikia, pengine wanalindwa, au wanaonekana kwamba wanadharau watu. Tutoe mawazo kama haya, maana wengi katika nafasi za mamlaka wana kiu ya kusikia Neno la Mungu ila hawajapata mtu wa kuwaambia.

Basi Yesu alikwenda pamoja na wazee, ila alipokuwa anakaribia nyumba, Yule akida alituma mtu kumwambia Yesu asisumbuke kuja kwake maana "sistahili Wewe uingie

chini ya dari langu, lakini sema Neno moja tu, na mtumwa wangu atapona; kwa maana mimi ni mtu wa mamlaka na huwaamrisha askari chini yangu waende hapa au wafanye hivi au vile" hivyo hakutaka awe kama anamwamrisha Yesu maana alijua Yesu ni BWANA anayewakilisha uwezo na nguvu za mamlaka yote ya mbinguni na duniani. Akajua chochote atakachosema kitakuwa. Alijiona amepungukiwa mbele ya BWANA na wala hakustahili aje nyumbani mwake. Japo wazee wale wa Kiyahudi walisema ni haki yake atendewe mema, kwa ajili ya kuwajali wao, yule akida alijua Yesu ni amiri Jeshi wa Malaika wasio na hesabu, na BWANA wa MABWANA wa majeshi yote, naye akajiona amepwaya sana.

Yesu alishangaa na kugeukia makutano waliomfuata akasema "sijaona imani kubwa namna hii Israeli." Hakika Akida huyu, mtu wa mataifa alikuwa tayari kumkiri Yesu na kushuhudia imani yake. Yesu asema tukimwonea aibu Naye atatuonea aibu, na tukimkiri Naye atatukiri mbele ya Babaye. Basi wale waliotumwa waliporudi nyumbani kwa akida walikuta yule mtumishi wake amepona saa ile ile Yesu alipomtamka; Ilikuwa saa saba Yesu alipotamka Maneno yale. Yesu alikuwa na mamlaka na uwezo wa mahali, muda na umbali. Pengine waliona wivu kwa mtu huyu wa mtaani, au wa mataifa kusifiwa vile, ila ndiyo ukweli wenyewe ulivyokuwa! Hata leo tunapojaribiwa kuwapendelea watu wa kabila, rangi au ukoo wetu, na kuwatenga wengine tujifunze kwamba kwa Mungu hakuna matabaka, tajiri au maskini, Mchina au Mwafrika, mnene au mwembamba. Wokovu ni wa wote na ni Yeye tu aweza kututoa, maana ni Baba yetu sote. Baada ya hapo Yesu alienda mji unaitwa Naini na hapa wanafunzi walifuatana Naye na akaona mkutano mkubwa ukikaribia lango la mji. Ulikuwa msafara wa kwenda kuzika kijana ambaye mama yake alikuwa mjane. Siku zile mjane alikuwa na shida kama hana watoto wa kiume, kwani aliweza kudhulumiwa, na asiwe na mahali pa kukaa au urithi wa ardhi ya kulima. Watu walikuwa wanamsindikiza mama huyu wakilia, kuonyesha huruma na upendo wao kwake.

Kijana huyu alikuwa mwana pekee wa mama yake au tumaini lake lilobaki, maana watoto ndiyo walitunza wazazi wao uzeeni au kwenye shida, hasa watoto wa kiume. Yesu alikaribia Jeneza kwa huruma akiona mama na ndugu zake wanalia, naye akaligusa Jeneza. Wale waliokuwa wakichukua maiti walisimama waone ni nini kitakachotokea. Naye akamwamrisha yule maiti "Kijana inuka." Watu kwanza walicheka, maana walifikiri, huyu Bwana hajui kwamba kijana amekufa; kisha vicheko vikakoma walipoona maiti hiyo inainuka na kuketi, hata kuzungumza. Biblia haisemi alisema nini, pengine alisema; mama unalia nini? Au mbona mnanibeba, au Asante Yesu kunipa maisha nimsaidie mama yangu. Hakika Yesu ni uzima na ufufuo, kila alipo kifo hakiwezi kuwepo.

Yesu anaonyesha huruma na rehema kwa watu walio na maumivu na shida. Basi akampa mama yake yule kijana, hofu ikawaingia wote na wakamtukuza Mungu wakijua nabii mkuu ametokea kwao na kuwaangalia watu Wake. Hawakujua kwamba Isa bin Mariamu ni zaidi ya nabii. Yaani ni Masihi, na Mwana wa Mungu. Habari hii ikaenea kote. Msafara ule wa huzuni wa watu wale, ukawa msafara wa kurudi toka makaburini mpaka nyumbani kwa yule mama huku kijana aliyekufa akiwa anatembea mwenyewe. Furaha iliyoje hiyo jamani! Wale wote ambao wamefiwa na

bibi, babu, mama, baba, wajomba na shangazi na marafiki wanaelewa jinsi uchungu wa kifo ulivyo.

Tunapopoteza tunayempenda kwa kifo, awe ni mzazi, mtoto au ndugu yoyote, tukumbuke ya kuwa Yesu ana nguvu leo kama zamani, alipozungumza na kijana wa Naini akimwambia ainuke. Atamwinua kila mmoja wetu toka kaburini siku moja atakapotokea mawinguni, kunyakua watu Wake, waishi milele zote. Siku zile waliofufuliwa waliishi miaka 70 au 50, ila wale watakaofufuliwa atakapokuja Mwana Adamu mawinguni sikuk ya hukumu, wataishi milele zote. Maneno Yake leo yanatufufua kutoka kwa vifo vya kiroho. Wengi wameacha imani, Shetani amewaua na dhambi. Leo tukiwa na imani ndani ya Yesu anatuambia tunyenyekee na kuacha maisha ya dhambi, Naye anatupa nguvu za kutembea tena. Macho yetu yangefumbuliwa leo tungejua Yesu anatuepusha na vifo na uovu mwingi kila siku, bila ya sisi kutambua.

*Wakati fadhaa zinatokea, na magumu yanakukabili, usitafute msaada kwa wanadamu. Muachie na kumtegemeaMUNGU kwa yote. Kitendo cha kuwaambia wengine shida zetu hutufanya tuwe dhaifu, na hakileti nguvu yoyote kwao. Kinaweka juu yao mzigo wa udhaifu wetu wa kiroho, ambao hawawezi kuutua. Tunatafuta nguvu kutoka kwa mwanadamu anayekosea, mtu mwenye mwisho, anayekufa, wakati tunaweza kuwa na nguvu ya MUNGU asiyekosea, na asiye na ukomo.
------------------------------


Maswali: Wazee walioishi na akida wa Kirumi walimwambia nini Yesu? Akida wa Kirumi alimwambiaje Yesu? Kwa nini mwanamke mjane alilia? Yesu alifanya nini aliposogea kwenye jeneza? Je kwa nini uzima wa milele ni muhimu? Maandiko yasema mtu akifa anaenda wapi? Tunaweza kusema mafarisayo walikuwa na shida, na masadukayo pia, ila watu wa mataifa kama Warumi walikuwa tayari kumpokea BWANA? Jadili hili!

**SIKU YA 221.**
**(Agosti 8)**

# Mariamu Magdalena na Marhamu ya upendo.

**Luka 7. Yohana 12.**

Mtu mmoja katika mafarisayo aitwa Simoni Mkoma, aliyeponywa ukoma na Yesu alimwalika Yesu aje kwake kula chakulawakaketipamoja.Watuwengi walikuwa hapa wakitaka pengine wamwone Lazaro aliyefufuliwa na Yesu au kumwona Yesu wamweleze shida zao. Kufufuliwa kwa Lazaro kuliwaonyesha wengi kwamba Yesu ni Masihi. Lazaro alikuwa ushahidi tosha wa ukuu wa Yesu, hata wengi yasemekana walitaka afe ili ushuhuda wa ukuu wa Yesu uyeyuke. Na tazama mwanamke mmoja alikuja mwenye dhambi ya ukahaba, alipata habari Yesu ameingia pale na ameketi chakulani kwenye nyumba ya Farisayo. Mwanamke huyu alileta chupa ya marashi au marimari yenye marhamu safi yenye thamani ya mishahara ya miaka mitatu, akitaka kuonyesha fadhila zake kwa Yesu.



Huyu alikuwa ametolewa na Yesu mapepo saba na Yesu alikuwa amemponya mwanamke huyu na kifo wakati alitaka kuuwawa kwa kupigwa mawe. Mwanamke huyu alikuwa yuko tayari kumfuata Yesu kokote alipoenda na kumhudumia, kwa kuwa alijua fika Yesu ni nani. Mwanamke huyu alipenda kumsikiliza Yesu, na kutaka kurudisha shukrani kwake. Akataka kuwa huru kutoka kwa Shetani na akataka kujitoa kikamilifu kwa Mungu. Huyu ni yule Yesu alimwambia aende na asitende dhambi. Hata sisi leo ikiwa Mungu ametutoa kwenye makucha ya Shetani, lazima tujisalimishe kwake kila siku, na kuwa na nia yake, tukifanya mapenzi Yake ili tusije tukaingia kwenye makucha ya Shetani tena.

Basi Mwanamke huyu Mariamu Magdalena, akasimama nyuma karibu na miguu Yake na kulia machozi ya shukurani. Akaanza kumdondoshea miguuni machozi yake, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake, akaibusu miguu yake na kuipaka ile marhamu. Pengine watu wengi wasingejua kinachoendelea, ila nyumba yote

ikajaa harufu ya marashi; na Yule farisayo Simoni, alivyoona vile, alisema moyoni mwake kuhusu Yesu "Mtu huyu angekuwa nabii, angemtambua mwanamke huyu amgusaye, ni nani, naye ni wa namna gani, ya kwamba ni mwenye dhambi. Watu wengine wakaanza kusema maneno, na mwanamke huyu pengine akasema "laiti ardhi ingepasuka, nitokomee maana nakodolewa macho sana hapa" akifikiria sijui Yesu atasemaje au Naye anaafikiana na Simoni?"

Yesu akiwa BWANA alijua yote awazayo akamwuliza "Simoni nina Neno nitakalo kukwambia." Simoni akashtuka kidogo na kusema sema mwalimu, ndipo Yesu akaelezea "kuna mtu mmoja mkopeshaji alikuwa na wadeni wawili, mmoja amwia dinari mia tano na wa pili hamsini. Nao walipokuwa hawana cha kumlipa aliwasamehe wote wawili. Katika hao wawili ni yupi atakayempenda zaidi? Simoni akajibu "yule aliyesamehewa deni kubwa." Basi Yesu akamwambia umeamua kwa haki, kisha akamgeukia yule mwanamke aitwaye Mariamu Magdalena na kumwambia Simoni "unaona mwanamke huyu? Niliingia nyumbani kwako, hukunipa maji kwa miguu Yangu; bali huyu amenidondoshea machozi miguu Yangu na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake. Wewe hukunibusu; lakini huyu tangu nilipoingia hakuacha kunibusu sana miguu Yangu. Hukunipaka mafuta; bali huyu amenipaka miguu Yangu marhamu.

Basi Yesu akasema, kwa ajili hiyo nakuambia, amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi, kwa kuwa amependa sana. Lakini amesamehewa kidogo, huyo ambaye hupenda kidogo." Hapa Simoni alijua Yesu ni BWANA kwani aliweza kusoma hata mawazo ya mtu. Simoni kwa destruri za kule alitakiwa kumtawadha miguu mgeni wake, kumpa salamu kwa busu, na vinginevyo ambavyo hakufanya. Simoni alipata muda wa kujichunguza, alifikiri anafanya heshima kumwalika Yesu, akakuta kwamba hata kwa dini yake, alikuwa hajamfanyia anavyopaswa kumfanyia kama mtu ampendaye. Simoni akagundua kwamba Yesu hakumwanika nje ubaya au dhambi zake; japo alizijua fika. Ila alitaka Yesu amwanike Mariamu nje; hili likamfanya ajione anawiwa. Mfarisayo huyu akawa mnyenyekevu. Yesu anapokea shukurani au zawadi yoyote tunayotoa, iwe ni maua aliyochuma mtoto njiani, au ni dhahabu. Yesu anapotukuta hatuachi tulivyo, anatusaidia kuwa watoto au watu bora zaidi ya alivyotukuta. Simoni naye hakuelewa upendo na rehema za Mungu akifikiri wenye dhambi wakosolewe papo hapo au waepukwe. Kisha akamwambia yule mwanamke "umesamehewa dhambi zako." Ndipo wale walioketi chakulani walianza kusema mioyoni mwao, "Ni nani huyu awezaye kusamehe dhambi?" Yesu akamwambia yule mwanamke, "Imani yako imekuponya enenda zako kwa imani."

Mwanafunzi wa Yesu Yuda Iskariote msaliti alipoona ile marhamu ilivyokuwa ya gharama alijisikia vibaya na kusema "mbona marhamu hii haikuuzwa kwa dinari mia tatu, wakapewa maskini?" Hata Mariamu pengine alianza kufikiri ndugu zake watamlaumu kwa kutumia pesa ovyo, wakijua; ila Yesu aliweka mambo yote sawa. Kwani Yuda alikuwa mwongo na mnafiki; hakujali maskini bali alikuwa mwizi, maana alikuwa mtunza hazina wa wanafunzi kumi na mbili wa Yesu na mara nyingi alikuwa anajilipa alipokuwa akifanya shughuli fulani, akidhania yeye ndiye aliyekuwa na elimu na maarifa mengi kuliko wenzake. Dhamira yake ilimshitaki kwamba yeye kama mtume, yuko tayari kumtendea hiana BWANA wake, ila wapita njia, wana

roho safi za kumfanyia makubwa Yesu.

Yesu hakumwaibisha Yuda mbele ya watu akijua uovu wake, nasi hili ni fundisho kwa watu tunaowajua ni waongo au wanafiki. Hatuna haja ya kuwaaibisha waovu mbele ya watu. Tuwaambie wakiwa peke yao na kuwaombea. Yesu akamwambia Yuda Israriote "Mwache aiweke kwa siku ya maziko yangu. Kwa maana maskini mnao sikuzote pamoja nanyi; bali Mimi hamnami sikuzote." Yuda alitoka nyumbani kwa Simoni baada ya tukio hili na kwenda kwa makuhani, kufanya njama ya kumwuza Yesu. Siku hii ndiyo alipokea vile vipande 30 vya fedha. Makuhani wale hawakuwa na upendo naye kama Yesu, na hawakutaka kabisa kuhusiana naye baada ya kumwuza Yesu. Nasi leo pia, Shetani na marafiki wabaya hawatupendi, na baada ya kututumia wanataka kutuondoa maishani mwao, tukiwa tumebaki kopo tupu. Thamani ya mwanadamu inaweza tu kupimwa na Mungu kwani Ndiye Muumbaji. Thamani ya mwanadamu inaweza tu kupimwa na Kifo cha Kristo, na sio mtu aliyeumbwa na anayekufa, hata awe Rais wa Nchi yangu kama Biden au Trump, au Obama, au Magufuli, au Kenyata.

Yesu Ndiyo Muumbaji na Mkombozi , Naye anajua thamani yetu ilivyo haswa. Sisi ni Wake kwa Uumbaji na Ukombozi, mara mbili! Nimesikia watu wengi ambao wana asili ya kiafirika napoishi wakisema mimi na nywele mbaya za kipilipili, za kiafrika. Siku moja tukiwa kanisani, Mchungaji mmoja akauliza ni nani hapa wanafikiri wana nywele mbaya. Karibu wote waliinua mikono, hasa wadada. Yule mchungaji akawauliza, nani amewaambieni nyie mna nywele mbaya? Muumba wenu amewaambia aliwaumba na nywele mbaya? Tulishangaa sana, maana toka udogo, wengi tumeambiwa, una miguu mibaya, una sura isiyopendenza, una masikio makubwa, umekonda mno, u mnene sana, u mfupi mno, shepu yako siyo namba nane, na hivyo tunaamini kwamba pengine tumeumbwa vibaya. Yale ambayo siwezi kuyaumba au kuyatengeneza, sina mamlaka nayo. Wazungu wanasema Mungu haumbi kitu duni (junk) au takataka. Leo jiulize maswali yafuatayo. Mimi ni nani? Nimeotaka wapi? Nipo hapa duniani kwaajili gani? na Ninakwenda wapi? Nawe utajitambua na hilo litabadilisha maisha yako. Mungu alituumba, sisi hatukujiumba wenyewe! Hakuna anayechagua aje duniani. Mungu anatupenda kuliko sisi tunavyojipenda wenyewe. Na wale tunaowapenda Yeye anawapenda kuzidi sisi. Kisa cha Mariamu kinaonyesha Mariamu alipojitambua yeye ni nani, aliendα kuishi maisha tofauti kabisa. Maswali haya nimejifunza kuyajibu katika kweli yote. Nitakupa majibu yangu. Mimi ni Gloria nimeumbwa na Mungu, niko hapa duniani kumpa utukufu Mungu, hiyo ndiyo sababu ya mimi kuwepo, dunia ilipoumbwa dhambi iliingia, na mambo yaliharibika na Yesu ikabidi aje ili kuyakarabati mambo kwa dhabihu Yake. Akachukua dhambi yetu, na kutupa maisha Yake, ili kuptia Yeye tuishi milele. Sasa najitayarisha kuelekea mbungini kwa neema ya Mungu, kila siku nasonga mbele, na siku moja nitaishi Naye milele zote. Mahusiano yale yaliyoharibika katika bustani ya Edeni kati ya mwanadamu na Mungu yatarudishwa, kwani tutaishi Naye milele zote, ambao ndio ulikuwa mpango Wake kabla ya mambo kuharibika. Hebu tembea na kuishi kama Mwana wa Mfalme wa mbinguni, hebu badilisha mtindo wako wa maisha na kumpa Mungu utukufu, na kumwuliza, Bwana unataka nifanye nini leo katika maisha yangu, Jibu litakuja kwa sala yako.

Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupatia ukamilifu wa baraka Zake. Ni nafasi ya upendeleo kwetu kunywa kwa kadiri tuwezavyo kutoka kwenye chemchemi ya upendo usio na kikomo. Kinachoshangaza ni kwamba tunaomba kidogo sana. MUNGU Yuko radhi na Yuko tayari kusikia maombi ya dhati ya watoto Wake walio wanyenyekevu zaidi Kwa nini wana na binti za MUNGU wanasita kuomba, wakati maombi ndiyo ufunguo katika mkono wa imani ili kufungua ghala za mbinguni, pahali ambako zimetunzwa hazina tele za Mweza wa Yote? Hebu usikose kwasababu huombi!

Huyu Mariamu Magdalena ndiye yule aliyekuwa na dada aliyeitwa Martha na kaka Lazaro aliyefufuliwa na Yesu. Kwa kutoa yale marhamu alileta furaha kwa Yesu, maana alimwonyesha amempokea na kumpenda akiwa hai, wakati aliokuwa akihitaji faraja sana, na wakati akiendea giza nene la mateso makuu. Mariamu hakujua kwa kikamilifu umuhimu wa lile tendo, maana alifanya tu kwa vile alimpenda Yesu aliyemwokoa, ila Roho Mtakatifu alimsaidia atende vile. Yesu alipofufuka kutoka kwenye mauti, Yeye ni harufu ya manukato kwetu sote. Hata leo tuwatendee watu mema wakiwa hai. Tusingoje wafe, ndipo tuweke maua makaburini.

Basi habari ya injili kokote ilipohubiriwa tendo la upendo la mwanamke huyu lilitajwa. Mwanamke huyu japo alikuwa mwovu, tendo hili lilionyesha kwamba anajutia dhambi zake. Tunamsoma leo kwa vile alikuwa ana moyo wa shukurani na ukarimu wa kupita mipaka, kwani zile pesa kwa leo zaweza kuwa kama dola 12,000 hivi au mamilioni ya shilingi. Baada ya karamu hii na ilipofika usiku Yuda alitoka kumsaliti Yesu. Japo alilalamika, kwamba Mariamu ametumia vibaya dinari 300 kumtayarisha Yesu kwa maziko, alikuwa tayari kupata pesa kwa kumwuza Yesu kwa vipande 30 tu vya pesa. Yuda aliwaambia makuhani usiku huu “Ni nini mtakachonipa nami nitamsaliti kwenu?”

Mariamu alienda na kuwa mwanafunzi wa Yesu, akasimama msalabani kuonyesha upendo wake, kisha akamsindikiza kaburini, na kuwa wa kwanza kumwona alipofufuka. Alipokea Roho Mtakatifu kati ya wale 120 siku ya Pentekoste. Yesu alikuja kuleta habari njema, kwamba ufalme Wake waja, basi tujutie makosa yetu na kutubu; tuyaache mambo ya zamani na kusafiri Naye siku kwa siku kama Mariamu. Yesu yupo tayari kupokea zawadi, hata kama ni ua toka kwa mtoto mdogo, au embe akijua kwamba inaonyesha upendo na heshima ya mtoto huyo. Yesu akujua hata wewe na mimi leo. Waweza kufikiri u mwenye dhambi, ila hata dhambi zako ziwe kubwa kiasi gani, hawezi kukufukuza, atakusamehe kabisa bila kukutoza chochote. Alikufa na kuchukua aibu, uchungu na uovu wa dhambi zetu. Anaishi kwa Baba mbinguni sasa kukuombea. Pata faraja kwa hilo. Na twende Kwake kwa ujasiri, na kumwambia tumekosa, Naye atatusamehe, na kutusaidia kuishi maisha mema.
Yaonekana hata wale Mamajusi wageni wa mbali walikuwa tayari kumpa Yesu zawadi na walimwamini akiwa mtoto mdogo, ila sasa akiwa mtu mzima na akiwa ametenda ishara zote, mitume Wake bado walikuwa wanasitasita kumwamini.

*Hauna haja ya kujipelekea au kusafiri huku na kule hadi miisho ya dunia ili kupata hekima, kwa maana MUNGU Yuko karibu nawe. Sio uwezo ulionao sasa au

utakaokuwa nao mbeleni, ndio ambao utakupa mafanikio. Ni kile ambacho Bwana anaweza kukufanyia. Tunahitaji kuwa na imani ndogo sana juu ya kile mwanadamu anachoweza kufanya na ujasiri mkubwa zaidi kwa kile MUNGU anachoweza kufanya kwa kila roho inayoamini. Anatamani mno wewe umuendee kwa imani. Anatamani sana utarajie kutoka Kwake mambo makubwa mno. Anatamani kukupa ufahamu katika mambo ya kidunia na pia katika mambo ya kiroho. Anaweza kuzinoa akili zako na zikawa bora zaidi. Anaweza kutoa busara na ustadi. Weka talanta zako katika kazi hiyo, mwombe MUNGU akupe hekima, nawe utapewa.

-------------------------

Maswali: Je Kwa nini Simoni mkoma alikuwa na mashaka na Yesu? Je Yuda Iskariote alikuwa tayari kuwapa maskini msaada? Mariamu alifanya tendo gani kuu? Je wewe leo wataka kumpa Yesu zawadi gani?

**SIKU YA 222.**
**(Agosti 9)**

# Marita na Mariamu dada wawili waliomshughulikia Yesu.

**Luka 10**



Ikawa katika kuenenda kwao, mitume na Yesu walifika nyumba ya marafiki zao Martha, na Mariamu. Hawa wakamfungulia mlango kwa furaha, kwa vile walimpenda Mwalimu huyu mashuhuri. Alipofika, shida zao zote ziliyeyuka mioyoni mwao. Mariamu Magdalena na dadaye na kaka yao aitwaye Lazaro, waliishi Bethania kama kilometa nne hivi toka mji wa Yerusalemu. Yesu alipenda kuja nyumba hii kutokana na urafiki na ukarimu wao. Hawa walikuwa wanafunzi wake pia. Walimfanyia Yesu ukarimu wa chakula na kumpatia mahali pa kukaa.

Huenda walishughulikia mambo yake binafsi kama kufua nguo na mambo mengine. Wana ndugu hawa walipenda Yesu awe mgeni wao, na wakafurahi kila alipokuja. Wakamhudumia, kwa kumpikia au huduma zingine tunazowapa wageni wapitao au wanaolala kwetu. Waweza kukumbuka huduma hizo ni zipi? Walikuwa wamemwamini Yesu, na Yesu alipoingia tu, watu walijazana kuja nyumbani kwao hivyo kukawa na wageni wengi wa kuwahudumia.

Martha anaonekana ndiye aliyekuwa mkubwa wao, au pengine mwenye nyumba hiyo. Martha akamkaribisha Yesu aingie kwao, au huenda walikuwa wamemwalika Yesu akipita mji huo akae kwao. Dada yake Mariamu badala ya kusaidiana na dadaye yake Martha kuwapikia wageni alijikalisha na wanaume sebuleni, lengo lake asikie Maneno ya matumaini ya Yesu. Martha akangoja Mariamu aje achochee moto au apike chakula lakini hakutokea. Wale wanafunzi 12 na wageni wengine waliendelea kuwepo sebuleni karibu na Yesu, wakisikiliza Maneno Yake na Mariamu akaburudishwa na Maneno ya Yesu.

Je hata wewe usingependa kukaa karibu na Mwalimu bora kupita wote duniani na kumsikiliza? Basi Martha alimwashiria Mariamu aje ila Mariamu alikuwa makini kusikiliza Maneno ya Yesu, hapo ndiyo Martha alikuja kulalamika mbele ya Yesu, maana akimwashiria alionekana kutopata ujumbe. Akasema mbona Yesu BWANA wa upendo na Mwalimu hajali, na dada mvivu huyu. Martha alimwaga mtama mbele ya kuku bila hata kuogopa, wasemee pembeni. Aliona Japo Yesu ana upendo, mbona anampendelea mdogo wake mariamu, akasema "BWANA hujali Wewe, au kuona ubaya hivyo ndugu yangu anavyoniacha nitumike peke yangu?"

Ukiangalia kweli, hata kwenye maisha ya leo, Martha alikuwa na sababu ya kweli, kwani wanaume zaidi ya 13 wakiingia nyumbani mwa mtu, na BWANA Mwenyewe Yupo wapaswa kushtuka na kuanza kuandaa maakuli. Pengine walikuwa hawajala kwa muda, nawe uanze kujikalisha tu, au kutegea kazi, halitakuwa jambo zuri au la busara. Ila Bwana akajibu akamwambia "Martha, Martha, unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi; lakini kinatakiwa kitu kimoja tu; na Mariamu amelichagua fungu lililo jema, ambalo hataondolewa."

Yesu alikuwa na shukrani kwa Martha kwa kuwa alikuwa anawatayarishia chakula, na kuwahudumia, maana alitambua inachukua muda kufanya haya, hasa kama hauna vifaa vya teknolojia vya gesi, umeme, au masufuria ya siku hizi vinavyorahisisha mapishi. Lakini alivutiwa pia na Mariamu aliyechagua kutafuta ufalme wa Mungu kwanza, kwa kusikiliza yatokayo kwa Yesu ambayo aliamini yatamsaidia katika maisha yake yote, ukilinganisha na chakula cha muda mfupi. Kila kitu kina sehemu yake, haikumaanisha asipikie wageni, la! Ila apange ili aweze kusikia Maneno toka kwa Mkate wa Mbinguni Mwenyewe au mana toka mbinguni.

Yesu aliwaambia Wayahudi nasi anatuambia leo kuwa Yeye ni Mkate wa Uzima na ambao ulikuwa pamoja na Wayahudi kwa muda mchache. Hivyo hivyo nasi leo, kuacha kwenda kanisani kusikia Maneno matakatifu eti tunapika na tuna wageni, ni sababu ambayo haina uzito. Mengine yaweza kuahirishwa kwa muda mchache. Martha alielewa kabisa Maneno haya, na nafikiri alishukuru, maana kujisahau kunatokea hasa kwa wakina mama wanapopika chakula. Ni kosa, kupika chakula na kuacha kuhudhuria ibada, kwa vile una wageni wengi. Tusizoelee tabia hiyo kamwe. Ni vyema kupanga mambo ili upate chakula au maneno ya uzima, maana chakula tunachokula kinatoka na kwenda jalalani. Upishi au kupiga deki, na kuosha vyombo vitakuweko kila siku, bali Maneno ya uzima ni ya milele. Tukumbuke, tuna muda mfupi wa kuyapokea kabla mlango wa rehema haujafungwa.

Kazi na michezo yetu ni vya muhimu. Ili mtoto akue vizuri apaswa acheze, maana hapo huigiza mambo ya kawaida ya maisha na kupata maana inayomsaidia kujua mambo yale. Ila pamoja na hayo, tusisahau kutafuta ufalme Wake, kwanza. Kabla hatujalala, tusome Neno la Mungu kwanza. Tumwombe Mungu na kumwuliza baraka. Na kabla hatujala chakula, tusome Neno la Mungu kisha tuombe. Ukifikiri hauna nafasi, fanya hivi, usile mpaka upate nafasi, hapo ndiyo utasikia njaa na kupata nafasi ya kusoma Neno la Mungu ili ule!

*Maombi na Imani vitafanya Mambo ya Ajabu — Ninaogopa kwamba hakuna imani hiyo ambayo ni muhimu na nyeti kuwa nanyo. Je! Hatuvaa njuga dhidi ya kukatishwa tamaa na vishawishi hata tuvunjike moyo? MUNGU ni Mwenye rehema, na tukifurahi katika Kweli, inayotakasa, nainayoboresha maisha, tunaweza kufanya kazi nzuri na thabiti kwa MUNGU. Maombi na imani vitafanya mambo ya kushangaza. Neno lazima liwe silaha yetu ya vita. Miujiza inaweza kufanywa kupitia Neno; kwa kuwa lina faida/manufaa kwa vitu vyote.

------------------------

Maswali: Kwa nini Martha alikuwa na mzigo moyoni? Kwa nini Mariamu alionekana kutojali? Kwa nini Yesu hakumkosoa Martha wala Mariamu? Kwa nini ni jambo jema kualika wageni? Je unasoma Neno la Mungu kabla ya kula kwanza? Twawezaje kuwa Mariamu kwenye ulimwengu wa Martha wenye shughuli nyingi?

**SIKU YA 223.**
**(Agosti 10)**

# Mpanzi au mpandaji mbegu, Yesu afundisha kwa mifano.

**Marko 3 na 4.**



Hata jamaa za Yesu walishindwa kuelewa kazi Yake na Uungu Wake. Kuna siku walienda kumkamata maana waliposikia habari toka kwa watu wengine walisema “amerukwa na akili.” Waliona atawapa shida na uongozi, kwani ameacha kazi nzuri ya useremala, anatembea na wanafunzi ambao nao ni wa ajabu, pia siku zingine anakaa bila kula na mengineyo ambayo waliona si ya kawaida kwa kibinadamu. Waandishi wakasema si Mwana wa Daudi huyu? Hawakugundua walimwita Jina Lake alilostahili na lililoko kwenye unabii. Hawakubisha kamwe, kwamba anatoka koo ya kifalme, walijua Masihi atakuwa Mwana wa Daudi bali kosa lao ni kwamba waliishia pale!

Walishangaa mtu bubu mwenye pepo aliweza kuzungumza na pepo walipomtoka, mtu huyu alimshukuru Yesu kwani alikuwa hajawahi kuzungumza toka utoto.

Alikuwa na shida, hata kumwita Yesu amwangalie ili amponye hatujui alifanyaje. Aliishi bila kusikia sauti ya mtoto wake akicheka, au akiimba. Alipoponywa, akaanza kusikia sauti za ndege wakiimba, sauti za watoto wakicheza na kukimbizana, hata majirani wakipiga vigelegele wakishangilia kupona kwake. Pengine maneno yake ya kwanza yalikuwa "Ahsante Yesu". Kushukuru ni jambo jema, na la muhimu. Alitaka azungumze mengi, kwani alikuwa ameweka maelfu ya maneno moyoni mwake, bila kuyasema. Sasa ulimi wake ulikuwa umefunguliwa.

Watu wengine badala ya kufurahi pia, waling'aka "anatoa pepo kwa Beelzebuli, yaani mkuu wa mapepo." Yesu aliwaambia yawezekanaje Shetani kumtoa Shetani. Ufalme wowote ukijipinga wenyewe hauwezi kusimama. Kama Shetani ameondoka na kujipinga mwenyewe basi hawezi kusimama bali kuwa na kikomo. Yesu alimaanisha kama Yeye na kazi Zake zatoka kwa shetani, basi inakuwaje anamtoa na kumfukuza Shetani aende, na mashetani wakikutana naye wanatetemeka na kuwa na hofu kama Yeye ni mwenzao? Mashetani walitaka watimue mbio walipomwona, na walimwomba ruksa waende kwenye nguruwe ili wapotee kwenye uso Wake. mashetani walitetemeka mbele Zake, ikionyesha wazi wazi, walikuwa hawataki kushirikiana Naye, au kuwa na urafiki wowote Naye.

Akiona kwamba maneno yao ni kufuru aliwaambia "Amini, nawaambia dhambi zote wanazotenda wanadamu watasamehewe, bali kukufuru Roho Mtakatifu, haina msamaha hata milele. Hiyo ni dhambi ya milele." Yesu alisema hivi waliposema ana pepo mchafu. Roho wa Mungu Ndiye anatujulisha tumekosa na kuomba toba – (Yohana 16:8). Endapo Roho wa Mungu hatumsikii, kwa kufa ganzi, na kuzoea uovu, sauti yake inazidi kuwa mbali na mwishowe, hakuna sauti tutakayosikia ikituambia hapa ni kosa, na hivyo tutaendelea kufanya uovu bila ya dhamira kutushtaki. Basi ikiwa unajiuliza kama umeshamkufuru Roho Mtakatifu, ujue hujafanya hivyo! Maana anayemkufuru Roho Mtakatifu huwa amefika hatua hajali chochote.

Yesu akawaambia "mtu asiye pamoja Nami, yu kinyume Changu, na mtu asiyekusanya pamoja Nami hutapanya." Mti mzuri hutoa matunda mazuri, ila mti mbaya una matunda mabaya, vivyo hivyo tabia za watu, kwani mtu hunena yale yaujazayo moyo wake. Yesu akasisitiza tusiseme ovyo ovyo bila kufikiri kwani "Kila neno lisilo maana, tukalolinena tutatoa hesabu yake siku ya hukumu." Waandishi wa mafarisayo walikuwa wamefikia hatua hii ya kutojiona wana dhambi. Usomapo hili, gundua kwamba unapofikiria tu kwamba umefanya dhambi isiyosamehewa basi ujue, hujaifanya, maana wale waifanyao wala hawafikiri vile. Mawazo yao yameenda mbali.

Hapo hapo waandishi wa mafarisayo walimwuliza awape ishara, Naye akawaambia, akasema kizazi kiovu chataka ishara, hata baada ya kuona makuu, basi ni ishara ya Yona tu ndiyo itakayowafaa. Akasema kwamba watu wa Ninawi watasimama hukumuni na kwenda mbinguni, ila wao hawatakwenda popote. Hata malkia wa Sheba (Ethiopia) atasimama kama mshindaji na kuwahukumu wao kwa kutoamini maana alimwamini Sulemani ambaye alikuwa binadamu aliyepewa hekima na Mungu na sasa Mungu Mwenyewe Yupo hapa ila wanazungumza hovyo ovyo tu, kwa kufuru.

Hawa wawili, walikuwa watu wa mataifa bali walisikia, na kwa imani wakabadilika. Ila Wayahudi walikuwa na Yesu BWANA Mwenyewe nao wasibadilike, kwa kutojali na kwa mawazo na maneno ya makufuru. Akawaambia kwamba pepo mchafu amtokapo mtu, na yule mtu asibadilike moyo; yule pepo huenda na kuchukua wenzake saba waovu zaidi, na hali ya yule mtu huwa mbaya zaidi kuliko awali. Ndiyo inavyokuwa mtu asiyetaka kusikiliza sauti ya Mungu. Basi walikuja mamaye na ndugu Zake na wakatuma mtu amwite, maana makutano walikuwa wengi wameketi kumzunguka. Pengine walikuwa wamesikia mafarisayo walivyokuwa wakizungumza Naye, Naye akiwajibu. Wakaona kwamba kwa vile wale ndiyo wakuu wa nchi wamwambie aachane nao.

Biblia haituambii, ila kila familia inapenda kumtembelea ndugu yao na kumpa mashauri fulani kule anakofanya kazi na kuishi. Ndugu Zake Yesu hawakuwa wameielewa kazi Yake sana. Badala ya wao kuwa faraja Kwake, mara zingine walionekana wanamletea maumivu, na ikawa rahisi Kwake kuwa mbali nao ili aweze kutimiza utume aliopewa na Baba yake. Ndugu Zake mara zingine walitaka kumbinafsisha awe kwa ajili yao tu na kufanya wanayotaka, au wamwamrishe cha kufanya. Walifikiri pengine wangemfundisha kuhusu Mungu na namna ya kuishi hapa duniani. Mara zingine walidhani anakuwa mwendawazimu, kama vile Feliki alivyomwambia Paulo "una wazimu" alipokuwa akifundisha Neno la Mungu.

Wengi hata siku hizi wanaomfanyia kazi Mungu kwa dhati, wakiwa hawana mshahara na kutia bidii ya kazi, wamehesabika kuwa wana 'kichaa'. Kukataliwa huku na kaka zake kulimfanya apende kuishi kwa rafiki kama Lazaro na kuwasiliana na Babaye kwa maombi. Mambo haya yalimpa faraja na furaha moyoni. Ila Yeye alisema "Mama Yangu na ndugu Zangu ni akina nani? Akajibu "ni yule atendaye mapenzi ya Mungu, ndiyo kaka Yangu, dada Yangu na mama Yangu." Yoyote yule apendaye baba yake, mama au watoto, kuliko Mungu, hawezi kufaa kwa huduma ambayo angemfanyia Mungu. Kufanya mapenzi ya Mungu, ndiyo kunakotufanya tuwe katika familia ya Mungu.

Je una furaha kwamba uko katika familia ya Mungu? Basi tunapewa faraja pale familia zetu zinapotutenga kwa kumpenda Yesu. Kumbuka hata Yesu ndugu Zake walifikiri anaenda kuharibu maisha Yake, wakifikiri wao wanajua kuliko Yeye! Japo kibinadamu twaweza tusijue kwa undani, ila kwa kuangalia kwa nje uhusiano kati ya Yesu na mama Yake uliokuwa wa muhimu kupita wote, ni kwamba alikuwa Mwokozi na Muumba Wake! Endapo angemkataa kama Mwokozi Wake, ingekuwa wazi kwamba angepotea milele.

Japo baadaye Yesu alipofufuka, walimkiri na kupata mafunuo hata wakaandika vitabu vya Biblia, Yesu alikuwa na wakati mgumu na nduguze mwanzoni. Hata leo japo tu wabishi na hatuelewi vizuri, bado tuna nafasi ya kumwambia ROHO wa Mungu asiyekosea atufunulie, ile Kweli, na kweli yote, na kutusaidia tuifuate, japo mawazo yetu yana mapokeo mengine. Tukiomba ombi hili, Yeye ni Mwaminifu na wa Kweli na atatuonyesha. Ila tusije kwa Mungu tukiwa na ajenda zetu, tukimwagiza tunachotaka. Bali tuende Kwake tukiwa wazi na tayari kufanya anachotaka, na

tukijitoa kikamilifu kufuata anachotuelekeza, hata kama kinapingana na mapenzi au desturi zetu.

Hata leo kuna wengi wanapata mateso, hasira na kukosolewa na watu wa karibu, iwe ndugu jamaa au marafiki. Hawa wajue watapata faraja wakikumbuka yale Yesu aliyopitia na kwamba si wao tu wenye shida hiyo ila kila mtu anayeamua kumfuata Mungu. Hawatakiwi kujiona kama watoto yatima, ila Baba yao wa mbinguni anajua yote. Yesu anaita watoto wote wenye kupata mateso, na kuwaambia, Yeye ni Baba yao, na anawapenda kuliko moyo wa binadamu yoyote anavyoweza kumpenda mtoto wake. Kwa kawaida Waisraeli waliouzwa utumwani, waliweza kukombolewa na jamaa zao wa karibu. Naye Yesu aliyetukomboa kutoka utumwa wa dhambi, amekuwa ndugu yetu, tena ndugu wa karibu kuliko baba, mama, kaka, dada au mpenzi yoyote. Hatuwezi kujua vizuri kuhusu upendo huu, ila tunajua kwamba ni upendo halisi, na kwamba twaweza kuwaonyesha wengine upendo huu.

Yesu aliwaambia mitume kwamba wao kwa vile waliacha baba, mama, jamaa na vyote, basi watapokea mengi ya thawabu kwenye ufalme huu wa duniani na ule wa mbinguni pia. Kila tunapojaribiwa kufikiri kwamba tumejitoa mhanga kumsaidia rafiki mwenye mahitaji, au kutoa kila kitu, na kuacha jamaa zetu ili tuwaite wengine kwa Kristo tusisahau kwamba Mungu si mdhulumaji, atatulipa haki yetu, na kama tunafikiri tumetoa zaidi kuliko tunavyopasa kutoa, tusijali, Yeye ni Mwaminifu atatурudishia chenji. Wakati huu Yesu alianza kufundisha kwa mifano na nje ya masinagogi au majengo. Mifano ya visa Vyake ilikuwa vitu au mambo ya duniani, vilivyo na maana ya mambo ya mbinguni. Mifano hii iliweza kuwaelewesha watu waliyoyajua na kuyaona, na kisha kuelewa yale wasiyoyajua.

Aliwafundisha mambo mengi kwa mifano. Akatoa mfano wa kilimo Akisema sikilizeni “Mpanzi alienda kupanda mbegu zingine zilianguka kando ya njia na ndege wakala. Zingine zilianguka kwenye mwamba pasipokuwa na udongo mwingi, japo ziliota, kwa vile jua lilikuwa jingi, na udongo haba mbegu iliungua kwa kuwa haikuwa na mizizi hivyo ikanyauka. Zingine zikaanguka miibani na japo ziliota miiba ikaisonga isizae matunda. Za mwisho zilianguka kwenye udongo ulio mzuri, zikastawi na kuzaa matunda. Mbegu moja ilizaa matunda 30, moja 20, moja 60, na moja 100. Akasema aliye na masikio ya kusikilia asikie maneno yale ya uzima. Alipokuwa peke yake na wanafunzi thenashara wakamwuliza maana ya ule mfano aliotoa. Naye akasema “Ninyi mmejaliwa kuijua siri za ufalme wa Mungu.”
Yesu alitoa mifano ili wale waliokuwa na nia ya kweli ya kuelewa wapate kuelewa ila wale wavivu au waliokuwa na kiburi yaliwapita hewani. Roho wa Mungu atawasaidia wale wanaotaka kujua Kweli, na wale wasiotaka kujua watakuwa kama wana masikio ila hawasikii, wana macho ila hawaoni. Yesu akawaambia udongo ni mioyo ya watu, mpanzi ni mtu anayewaambia watu habari za wokovu kutoka kwenye Maandiko. Mbegu ni Neno la Mungu au habari njema.

Mbegu zilizoanguka barabarini zawakilisha wale waliopata habari njema ila Shetani akaja kuchukua Neno lililopandwa mioyoni mwao. Wale wapandwao kwenye miamba ni wale ambao walipolisikia Neno walilipokea kwa furaha ila halikuenda ndani ya mioyo yao na hivyo likakosa mizizi. Hawa ni wale ambao hukaa na Neno

kwa muda mchache na yakitokea mateso, dhiki au udhia kwa ajili ya lile Neno hujikwaa.

Na wale waliopandwa kwenye miiba ni watu wanaolisikia Neno na mahangaiko, shughuli za dunia, udanganyifu wa mali na tamaa za mambo mengi huwashika nazo hulisonga lile Neno likawa halizai. Na wale waliopandwa kwenye udongo mzuri, ni watu walisikiao Neno na kulipokea, na kuzaa matunda 30, 60, na 100 kwa utukufu wa Mungu. Hebu tusikate tamaa tupandapo. Endapo tupo tayari kupanda, lazima tutavuna. Mianzo midogo ya mbegu ndogo huleta matunda makubwa mazuri. Udongo ndiyo kikwazo cha matunda kuwa mazuri. Zote ziliota, ila hazikuzaa, ikimaanisha moyo ulikuwa na hitilafu.

Akawaambia hakuna lililositirika ambalo halitadhihirika, au lililofichwa ambalo makusudi yake hayatakuwa wazi. Yesu aliwaambia, kile "mpimacho ndicho mtakachopimiwa, na tena mtazidishiwa, kwa maana aliyenacho ataongezewa naye asiyenacho atanyanganywa hata kile alicho nacho." Basi leo hatutaki kunyanganywa kile Mungu alichotupa. Tunaomba atupe nguvu tuzae matunda ya upendo, furaha, uvumilivu, amani, na utu wema.


*"Usichanganye imani na hisia pamoja. Vipo tofauti. Tunapaswa kuwa na imani. Imani hii lazima tuifanyie mazoezi. Amini, amini. Hebu imani yako ishikilie baraka, na ni zako. Hisia zako hazina uhusiano wowote na imani hii. Imani inapoleta baraka moyoni mwako, na unafurahi katika baraka, sio imani tena, bali ni hisia. —(Testimonies for the Church 1:167.) Maombi na Imani vinashikilia Nguvu za MUNGU- Imani ya kweli na ombi la kweli — vina nguvu kiasi gani! Ni kama mikono miwili ambayo mwanadamu mwombaji hushikilia nguvu ya Upendo usio na kipimo.
---------------------------

Maswali: Wayahudi walisema Yesu ana mashetani alipofanya jambo gani? Nini maana ya Shetani hawezi kumtoa Shetani? Mama na ndugu za Yesu ni nani? Je wewe ni ndugu ya Yesu leo? Mbegu zilizotoa matunda zinawakilisha nini? Kumkufuru Roho Mtakatifu kuna maana gani? Mbegu za Mpanzi ziliangukia sehemu gani? Sehemu hizo zinawakilisha nini? Soma zaid kwenye kitabu kinachoitwa Lulu za Uzima, hiki kimeelezea mifano ya Yesu kwa kinagaubaga zaidi!

**SIKU YA 224.**
**(Agosti 11)**

# Mifano ya Yesu. Upepo wamtii.

**Marko 4. Mathayo 8.**



Yesu akifundisha kwa mifano, alianza kwa kutoa mfano wa kilimo. Akasema ufalme wa mbinguni ni kama mtu aliyemwaga mbegu ardhini, na alipolala mbegu ikaanza kumea kwa namna asivyojua yeye kueleza, kuanzia kuota hata kukua, maana ni Mungu pekee ajuaye. Ila kuna mwingine akapanda magugu, hivyo majani na mbegu ya chakula vikakua pamoja. Mtumishi akauliza kama ang'oe magugu, akaambiwa la! Angoje mpaka yakue ndipo tofauti itaonekana ya hiyo miche.

Majani yakatokea kisha masuke, na ikafika siku akapeleka mundu kuvuna alichopanda. Siku hiyo akatenganisha ngano na magugu. Ngano ikimaanisha wale wanaomtii na kuwa na imani Naye, magugu ni wale waovu. Yale magugu hayatakuwepo mbinguni, kwani yalichomwa moto. Magugu ni watu wanaoendelea katika njia zao, wasijisalimishe kwa Yesu. Je unafikiri kuna mtu anataka kuwa magugu?

Unaposhangaa kwa nini watu wengine kanisani wana tabia ambazo zinafanya ujiulize maswali. Unajiuliza inakuwaje watu wengine wanaosema wanampenda Mungu

hawana upendo? Unagundua kwamba huenda hawa ni magugu, ila usiwahukumu, bali acha Mungu mwenyewe awahukumu. Yesu akimwita mtu, anataka afe kwa mambo yale ya maisha ya mwanzo.
Kisha Yesu akatoa mfano mwingine "Tulinganishe ufalme wa Mungu na nini? Ufalme wa Mungu ni kama punje ya haradali ambayo ikipandwa mbegu yake ni ndogo sana kupita zote zinazopandwa. Hii ikakua, na kuwa kubwa kuliko miti yote ya mboga, na kufanya matawi makubwa, hata ndege wa angani waweza kukaa chini ya uvuli Wake.

Basi kwa mifano mingi ya namna hii, Yesu Mwalimu mkuu alifundisha. Tabibu Luka amerekodi mifano 19 hivi. Yesu, alikuwa akisema Neno Lake, kwa mifano, na wala hakusema pasipo mifano. Lakini aliwafanunulia wanafunzi Wake na watu waliokuwa wanyenyekevu na waliofundishwa Naye, mambo yote kwa faragha. Aliwaelezea jinsi ile mifano inavyohusiana na mambo ya ufalme wa mbinguni. Wale wanyenyekevu wote ambao walikuwa wamemimina roho zao wapate kulisikia na kulitii Neno walibadilishwa na mafundisho Yake kwa njia za ajabu.

Muujiza mkubwa kupita wote wa Mungu ni kutusamehe dhambi na kutusaidia tuishi maisha ya ushindi. Mifano hii ilisaidia kuyafanya mafundisho Yake kueleweka kwa watu. Mbili ya tatu ya mifano hii, ilihusu fedha au mali. Yesu alifanya hivi kudhihirisha pale moyo wa mtu ulipo. Moyo wa mwanadamu upo kwenye hazina Yake; yaani kwenye kile kinachoteka akili yake sana ambacho ni fedha au uchumi!
Siku ile kulipokuwa jioni akawaambia wanafunzi wavuke ng'ambo na wakaacha makutano, na wakaenda Naye kwenye vyombo vyao. Basi ikatokea dhoruba kuu ya upepo na mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji. Naye Mwenyewe alikuwa mwishoni mwa mashua amelala juu ya pilo, kwa amani. Wanafunzi wakiogopa walimwambia kwa hofu "BWANA tuokoe tunaangamia, si kitu kwako tunaangamia?" Yesu aliamka bila haraka au hofu na kuukemea upepo, akiiambia bahari "Nyamaza utulie." Uumbaji unajua sauti ya mkuu Wake; upepo, mapepo, maji, mimea, na viasili vyote vinamtii.

Akawaambia wanafunzi "mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado?" Wanafunzi wakaingiwa na hofu kuu, wakaambiana "Ni nani huyu, basi hata upepo na bahari humtii?" Wakaanza kuelewa kwamba huyu ni Mungu pamoja nasi, kwani ni Mungu tu Mwenye uwezo wote. Kwa kweli wanafunzi walikuwa kwenye shule kubwa kupita zote zilizokuwako au zitakazokuwako kwani walikuwa na Mwalimu mkuu kupita wote. Mungu alikuwa akiwafundisha uso kwa uso. Nimewaza mara nyingi kama ningepata nafasi kama yao! Walijenga tabia zao juu ya msingi wa Kristo, ili wasaidie wengine na kisha wao, na hao wengine wapate uzima wa milele. Wanafunzi walikuwa wameona mengi, ila bado walikuwa wanasahau wakifikiri ni binadamu mwenzao; ndiyo alikuwa binadamu, ila alikuwa Mungu pia, kamwe hajaonekana mtu kama huyu, wala hatatokea mwingine kama huyu aliyekuwa Mungu na tena binadamu.
Hata leo Yesu anatuliza dhoruba za mioyo yetu. Katika dhoruba zote, mwambie Yesu moyoni mwako "BWANA niokoe", ataleta wokovu kwako. Mara zingine yaonekana kwetu kama 'amelala' na hajali wakati tukiwa uso kwa uso na hatari. Hebu katika hali zote, ana uwezo na mamlaka ya kuokoa.

*Kwa unyofu wa moyo, katika njaa ya kiroho, mlilie MUNGU. Shindana na mawakala wa mbinguni hadi upate ushindi. Wekeza mwili na Roho yako yote mikononi mwa Bwana, nafsi, mwili, na roho, na amua kuwa, wakala Wake mpendwa aliyejiweka wakfu, akiongozwa na mapenzi Yake, akidhibitiwa na akili Yake, na kujazwa na Roho Wake.

---------------------------------

Maswali: Magugu ni nini na mazao mazuri ni nini? Kwa nini upepo ulitii sauti ya Yesu? Punje ya haradali inafananishwa na nini? Kwa nini mifano ya Yesu mingi ilihusu mali au fedha? Kwa nini Yesu alizungumza kwa mifano? Kwa nini uzoefu wa maisha ya kila mtu ni shule ya kujenga tabia ili afanane na Kristo?

**SIKU YA 225**
**(Agosti 12)**

# Mitume 12 waenda kazini.

**Mathayo 10, Luka 9.**



Ulipofika wakati wa Yesu kuzaliwa, Waisraeli walikuwa wamejichanganya na watu wasioamini au kupenda mambo ya Mungu. Walikuwa wamechukua mapokeo, desturi na imani zingine ambazo ziliwafanya wasiwe waaminifu kwa Mungu. Hata mafarisayo waolikuwa na Maandiko ya ile Kweli walijiingiza kwenye unafiki au uchakachuaji. Yesu alianza kupalilia kanisa upya na mitume ndiyo walikuwa wafuasi wa kwanza. Yesu alipochagua mitume alichukua muda kuunda kulipanga kanisa kama taasisi, ili atakapoenda mbinguni waendelee na kazi.

Mitume ndiyo viongozi wa kwanza wa kanisa la Kikristo, na vizazi vinavyofuata mpaka leo. Sisi tunasimama kwenye mabega ya watu hawa, nasi sote tunasimama kwenye Msingi mkuu ambao ni Yesu. Kanisa hili la mitume, lilifanya kazi kwa uaminifu, kwa kutoa mafundisho ya ile Kweli. Nasi pia leo kama Wakristo, twapaswa tufuate yale yote waliyoandika na kutuachia, mpaka siku ile ya asubuhi njema Yesu atakapotokezea mawinguni na parapanda, pamoja na malaika akija kutuchukua tuishi Naye milele zote. Hawakuwa na majengo ya ofisi au kanisa la kukutania ili

wapange utume. Walifanyia shughuli zao kwenye milima, majini na mahali pa wazi. Waliona mengi ya uumbaji kama mawingu ya bluu, majani ya kijani na mioyo yao ikatulizwa walipomsikiliza Mwalimu wao akitoa mifano.

Yesu Alijua udhaifu wa kila mwanafunzi. Wanafunzi wengine walitaka kuwa na madaraka, wengine walikuwa na hasira za haraka, na wengine hawakufurahia mambo yalivyokuwa yakiendelea chini ya utawala wa serikali ya Warumi. Walisafiri na kuishi na Yesu kwa miaka hiyo mitatu na nusu wakijifunza jinsi ya kuokoa watu. Yohana aliyekuwa mdogo kwa wote, na aliyependa kukaa karibu na Yesu, anatupa picha ya kina ya uwezo wa Mungu katika kubadili hasira zake kuwa upendo. Hatusomi mahali ambapo Yesu alimwita Yuda ajiunge na kundi lake. Huenda alijiunga akitaka nafasi ya madaraka 'kwenye serikali' itakayoundwa baada ya kuwatoa Warumi. Yesu hakumfukuza, na watu walimwona ni mtu mwema tu, anayemfanyia kazi Mungu kumbe maskini alikuwa mbali na nia hiyo.

Yuda alikuwa na ubinafsi na tamaa ya mali, lakini Yesu alimpa nafasi ya kubadilika, endapo angechagua. Yesu aliwarudi mitume walipokosea, ila hawakukwazika na kujiunga na kundi lingine. Jinsi walivyokuwa karibu na Yesu ndiyo walikuwa karibu na mitume wenzao, wakiafikiana kwa yale wafanyayo. Yesu hakuwapanga malaika wafanye kazi ya kuokoa binadamu. Kazi hiyo walipangiwa wanadamu kama wewe na mimi. Tabia zetu japo mbovu, Yesu Yupo tayari kutufundisha ili tuwe kama Yeye. Yesu aliwasaidia mitume kuelewa ufalme Wake si wa kuangusha Rumi, bali ulikuwa na ukuu zaidi ya mambo ya taifa moja.

Yesu hakuponya wagonjwa na kutoa pepo mwenyewe tu, bali aliwapa wanafunzi mamlaka ya kufanya hivi pia. Wote kumi na mbili walitoa mapepo na kuponya wagonjwa. Mitume wakawa wahubiri na matabibu pia. Yesu aliwatuma hawa thenashara, akiwaagiza wasiende kwa mataifa au mji wa Wasamaria bali waanzie kwa watu wa karibu kwanza, yaani kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Akawaambia wakienda wahubiri, wakisema "ufalme wa mbinguni umekaribia." Waponye wagonjwa, wafufue wafu, watakase wenye ukoma na kutoa pepo. Wasitoze watu kwani wamepata bure na watoe bure hicho kipaji. Akawaambia wasichukue dhahabu, fedha, pesa, mkoba, kanzu mbili, fimbo au viatu, maana mtenda kazi anastahili posho yake. Wakiwapelekea watu habari njema, watu hao wapaswa kuwapa mahitaji yao.

Akawaambia wakiingia kijiji chochote watafute mtu mwaminifu na mkarimu wakae kwake hata watakapotoka. Na wakiingia katika nyumba wasalimu watu, na kama ile nyumba inastahii amani yao, basi amani itaifikia la haistahili amani basi amani hiyo itawarudia wao. "Mtu asipowakaribisha na kuwasikiliza maneno yenu ya habari njema, mtokapo katika nyumba ile, au mji ule kung'uteni mavumbi ya miguuni mwenu." Hiyo itawatambulisha kwamba tendo lile walilofanya si jema au la baraka kwao na ya kwamba walipata nafasi ya kusikia habari muhimu kupita zote, ila walizipuuza. Maana itakuwa rahisi kwa miji miovu ya Sodoma na Gomora kustahili adhabu siku ya hukumu kuliko ile Miji ambayo haitaki kupokea habari na Neno la Mwenyezi Mungu.

Mitume walipewa mamlaka na uwezo wa kufanya vitu vikubwa; ila Yesu aliwatahadharisha dhidi ya masadukayo, mafarisayo na makuhani, na baraza la wazee. Yesu akasema anawatuma wao kama wanakondoo kwa mbwa mwitu, maana watu wengi ni wapenda uovu, na hawataki kusikia habari za Mungu. Akawatahadharisha kuwa na busara kama nyoka na kuwa wapole kama njiwa. Akawaambia wajihadhari na wanadamu maana watawapeleka mahakamani na kwenye masinagogi na kuwapiga, nao watachukuliwa mbele ya sheria na mbele ya wafalme kwa ajili ya Yesu kuwa ushuhuda kwao na kwa mataifa. Hata leo mamilioni ya waumini wanapitia mateso hasa zile nchi za dirisha la 1040 (latitude, longitude) kama Korea ya Kaskazini, Somalia na zingine nyingi. Angalia ramani uone hilo dirisha! Twapaswa tuwakumbuke hawa katika maombi yetu. Kuna nchi zingine zinapitia vita na hii inasitisha ibada za jumla kwa waumini wengi.

Hivi ndivyo watu wa ngazi za juu watakavyopata nafasi ya kusikia ili wajitayarishe kwa ufalme wa Mungu. Ila watakapowapeleka "msifikiri fikiri jinsi mtakavyosema" maana Mungu ataweka midomoni mwenu cha kusema, itakuwa si nyinyi mnazungumza bali Roho wa Mungu atakuwa anasema ndani yenu. Hapo ndipo ndugu atamsaliti mwenzake, ili auwawe. Baba atamsaliti mwana, na wana watainuka kinyume cha wazazi na kuwaua. Mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya Jina Langu. Ila mwenye kuvumilia mpaka mwisho ndiye atakayeokoka. Ila watakapowafukuza kwenye mji mmoja, kimbilieni mji mwingine kuwaambia habari njema za ufalme na Hukumu ya Mungu inayokuja. Yesu akawaambia "hamtaimaliza miji yote hata ajapo Mwana wa Adamu."

Mwanafunzi hampiti mwalimu wake au mtumwa hampiti bwana wake. Yamtosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu Wake. Ikiwa wamemwita Yeye Yesu Beelzebuli, Je si zaidi wale wafuasi au wanafunzi Wake watakavyotendewa maovu? Akawaambia wasiogope maana hakuna lililofichwa, ambalo halitajulikana. Lolote ambalo atasema nao kwenye giza waseme nuruni, na wasikialo kwa siri, wahubiri juu ya jukwaa kila mtu asikie. Wasiwaogope wale waovu wauao mwili kwani hawawezi kuua roho. Afadhali kumuogopa yule awezaye kuangamiza mwili na roho katika hukumu ya Jehanamu itakayotokea mwisho wa dunia.

Mitume wakatoka kwenda miji yote katika sehemu hiyo wakahubiri wakiponya kila aina ya magonjwa. Alipowaambia amewapa mamlaka ya kushika nyoka asiwadhuru, na kunywa sumu wasife, hakuwa na maana waende washike nyoka porini ili waone uwezo wao, au wanywe sumu kwa makusudi watu waone jinsi walivyo na uwezo. La! alisema kama imetokea kwamba mambo haya yamewapata, na kwa bahati mbaya wameumwa na nyoka katika shughuli ya kueneza Neno la Mungu, au wametiliwa sumu kwenye chakula na mtu kwa hila mbaya hivi vitu havitawadhuru.

Miaka ya 1,800 watu walikuwa wanashika nyoka na kunywa sumu, wakisema Mungu atawasaidia. Huu ni upuuzi na kwenda nje ya maana iliyokusudiwa. Mfano mwingine unaofanana na huo ni hapo aliposema jicho lako likikukosesha ling'oe ulitupe. Hili nalo watu wakilichukua hivyo lilivyo basi dunia itakuwa ni ya vipofu, na bado watu wataendelea kufanya dhambi hali ni vipofu.

*Mwambie Yesu matakwa yako kwa unyofu wa roho yako (kwa dhati). Siyo lazima ufanye mabishano au mjadala mrefu Naye, au kumhubiria MUNGU, lakini kwa moyo wa huzuni kwaajili ya dhambi zako, sema, “Niokoe, Bwana, la sivyo nitaangamia.” Kuna matumaini kwa roho kama hizo. Watatafuta, wataomba, watabisha, na watapata. Wakati Yesu ameondoa mzigo wa dhambi unayousagasaga moyo, utaburudishwa kwa baraka ya amani ya Kristo

-------------------------------

Maswali: Kwa nini Yesu hakumfukuza Yuda japo alijua moyo wake? Kwa nini tusifikirie tutakayozungumza tukipelekwa kortini? Kwa nini Yesu alisema mwanafunzi hampiti Mwalimu wake? Kuna tofauti gani kati ya kanisa la makuhani wale kama Anasi na kanisa la mitume Yesu aliloanzisha?

**SIKU YA 226.**
**(Agosti 13)**

# Kutuma wanafunzi 70 umishonari.

**Luka 10.**

BWANA Yesu alikusanya wanafunzi 70, kando ya wale 12 na kuwatuma wawili wawili wamtangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe. Hii ilisaidia kurahisisha kazi, na kufanya watu wawe wameelewa vizuri habari za Mungu ili wakatishwe shauri wakijua vizuri habari njema. Akawambia hawa sabini "Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache, basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno Yake'. Hata leo mavuno ni mengi; watu wengi wako tayari kupata habari za ufalme wa Mungu unaokuja siku za karibuni, ila watoto kwa watu wazima wana shughuli nyingi, au hawatilii maanani. Ila ni amri kwetu hata kama hatuwezi kufanya vingi, kusali kwa dua na kuugua kuombea BWANA alete watenda kazi kuvuna shambani Mwake. Kila mtoto, mtu mzima na hata mzee aweza kufanya hilo.

Akawaambia anawatuma kama wanakondoo kati ya mbwa mwitu, wasichukue mfuko, mkoba, au viatu. Kuna wengine ambao walikuwa wana hila na kupenda kupinga nuru kwani Shetani aliwatumia, ila nje walionekana watu wema tu hawa ndiyo walikuwa mbwa mwitu. Wengine walikuwa wapelezi kati yao watu ambao hawakunuia wema wakitaka kuwapeleka gerezani. Mitume waliambiwa yoyote anayewapokea ni sawa na kumpokea Yeye Mwana wa Mungu au Baba wa mbinguni. Wakaagizwa wasisalimu watu njiani huku na kule na kuhadithiana hadithi nyingi au kupiga umbeya kupoteza muda maana shughuli yao ni ya dharura hivyo wasipoteze dira au lengo lao. Na nyumba yoyote waingiayo wabariki "amani iwemo nyumbani humo"mkiwaonyesha nyinyi ni watu wa amani wenye nia njema kuwasaidia maisha yao kwa vile vya milele.

Kama wenyeji wenu wakiwa ni watu wasiotaka kujifunza Neno la Mungu na wanaleta shida, mtatoka na amani yenu itarudi kwenu. Mkipata mtu mwema aliye tayari kusikia habari za ufalme wa Mungu, kaeni pale mlipokaribishwa mkinywa na kula maana mtenda kazi amestahili ujira wake. Msihame hame toka nyumba moja kwenda nyingine mtaonekana na wenyeji wenu kama mnaotaka kukidhi matakwa yenu au ni wagumu kuishi na watu. Ila mwendelee kufikia wengine kutoka kituo hiki kimoja. Mji wowote mkiingia mkakaribishwa, mle na kufanya huduma zote za kuponya wagonjwa waliomo, mkiwaambia "ufalme wa Mungu umekaribia."

Ila wale wasiowakaribisha, tokeni humo nanyi mkipita katika njia zake semeni tunatoka maana hatutakiwi humu, mkung'ute mavumbi ya miguu yenu. Lakini jueni hili kwamba "ufalme wa Mungu umekaribia." Itakuwa rahisi kwa Sodoma na Gomora ile ya kiyama au hukumu kuistahimili adhabu yake kuliko mji au yule mtu anayekataa Neno la Mungu. Mtu anayewasikiliza watumishi hawa wa Mungu atakuwa anamsikiliza Mungu ila yeye anayekataa atakuwa anamkataa Mungu pia.

Wale 70 walirudi baada ya kazi hiyo na kwa furaha, wakisema "pepo wanatutii." Yesu akawaambia "Nalimwona Shetani akainguka toka mbinguni kama umeme." Akawapa amri ya kukanyaga nyoka na ng'e na nguvu zote za yule adui "wala hakuna kitu kitachowadhuru." Akawaambia wasifurahi kwa vile pepo wanawatii bali wafurahi kwa sababu majina yao yameandikwa mbinguni. Maagizo ya wanafunzi 70 yalifanana sana tu na yale ya wale 12 walipotumwa.

Wainjilisti hawa wa kwanza, ni mfano wa kila anayempenda Mungu leo, mtoto na hata mkubwa. Yesu alipoenda mbinguni mitume walijikuta wanakumbuka yale maagizo Yake, wakaleta yale mafaili kutoka vichwani mwao na kuwaambia watu yale maneno aliyosema. Yesu alitumia muda mwingi kuponya watu zaidi ya kuhubiri, sauti Yake ilikuwa ya kwanza kusikiwa na viziwi wengi, na uso Wake wa kwanza kutazamwa na vipofu aliowaponya. Alikuwa kama mwali wa kuleta furaha. Hata leo kazi ya uinjilisti yapaswa kuwa na mafanikio Yake. Tufanye kama Yesu alivyofanya kuwalisha wenye njaa, kufariji wenye huzuni na kuwapa matumaini wale waliokata tamaa.

Mitume walienda miji ya watu, wakivaa nguo za watu wa kawaida; kwenye nyumba hizi waliwaambia watu habari njema wakaomba nao na kusoma Maandiko, wenye shida waliletwa na kusaidiwa. Mitume walifurahia kipaji cha kuponya na kuhubiri, hawakufikiria sana mateso. Ndipo Yesu akasema anawatuma kwenye mbwa wa mwitu, ila wawe na hekima kama Nyoka ila wapole kama njiwa. Yesu hakuwa na Jeuri au kuumiza watu kwa maneno Yake bila ya kuwa na sababu.

Tuepukane na kubishana na watu ili tuwashinde, au ili waje kwenye dhehebu letu. Lengo letu kubwa ni kusaidia roho ile iongoke, kisha roho hiyo isome Maandiko na kuyafuata, bila kusikiliza mapokeo ya binadamu. Maneno ya upole ya Yesu ndiyo yanayoshinda, siyo nguvu zetu au uwezo wetu wa kujadili. Siku zingine wengi walisikia kwenye taarifa ya habari Rais wa Marekani Bush na Rais wa Iraki Sadam wakisema wanamtetea Mungu. Mungu ana uwezo tosha wa kujitetea na wala hahitaji watu wamtetee. Hebu tusiwe watu wa kujibishana kwa jeuri tukitamba na kuwa wakatili kama Goliati. Dini ya Kweli ya Kristo ni ya upole, na si ya mashindano. Tunaweza tushinde pigano hilo la malumbano, ila tusishinde vita, adui wetu ni mjanja, anataka tuwe kwenye mizozo na kusahau lengo letu. Ukristo ni Mungu anamtafuta mwanadamu kwa upendo wote, na dini ni mwanadamu anamtafuta Mungu, kwa njia ambazo zinaweza kuwa za kweli au za uongo. Masihi Ndiye anatusaidia kuipata Kweli yote, si dini au viongozi wake. Yesu ni Njia Kweli na uzima. Dini ni ushirika unaotusaidia kufarijiana katika safari ya kwenda mbinguni tukiwaita watu kuingia katika safina ya kwenda mbinguni. Yesu anataka hata leo, tusiwe na hofu na kujibidisha kukariri, kwamba tupelekwapo magerezani au kwa wakuu tutajibu kwa namna fulani. Yeye anatupa Maneno ya kushuhudia ili wafalme na watu wenye nafasi wamwamini Yeye. Ila inatubidi tusome Maneno haya na kuyajua maana hatuwezi kukumbushwa vile ambavyo hatuna thamani navyo kuvisoma.

Twapaswa tufanye hivi kwa unyenyekevu na Roho Mtakatifu atayaleta mafaili ya Maandiko yaliyo kichwani kwenye midomo yetu. Yesu aliwatahadharisha kwamba hata familia zao zitawachukia. Hakuwatuma kujiletea majaribu au mateso. Yesu

aliwapenda binadamu wote ila alikuwa rafiki wa Kweli, asiyenyamza wakati mtu akifanya mipango ya kujiangamiza na uovu. Wote wanaompenda Mungu tusijali amani na maelewano zaidi ya kufuata kanuni na Maandiko ya Mungu. Akasisitiza hata wanaoua wasiogopwe maana wanaua mwili tu na si roho. Kumshuhudia Yesu kwa wengine ni zaidi ya kujua tu mafundisho Yake, bali ni kuwa na upendo wake kwa watu, na kuwajali. Twaweza kutoa picha mbaya ya Yesu kwa kusema uongo, kuzungumza kwa jeuri, kuwa wachoyo au wavivu.

Yesu alijua kuwa mfuasi Wake wakati wa kipindi chochote kile cha historia ni kutangaza vita; kwa vile Shetani anataka daima kupigana vita na ufalme wa Mungu. Aliahidi wote wanaowatendea vyema watumishi Wake, itakuwa ni kama wamemtendea Yeye Mwenyewe. Yohana anatuambia walijifunza mengi mno, hata bahari ingekuwa wino, mbingu ziwe karatasi na miti iwe kalamu, na kila mtu awe mwandishi bado isingetosha kuelezea yote waliyojifunza. Mitume walipotoa tarifa ya mafanikio yao, Yesu aliwachukua faragha ili waombe. Walikuwa wamekaa na watu, waliohitaji huduma. Walikuwa hawajala wala kushughulikia mahitaji yao ya mwili. Walihitaji mafunzo zaidi ya kuwafanya kuwa wanyenyekevu, kwani kulikuwa na hatari kule kuona mapepo yakiwatii kungewafanya waote mapembe.

Walihitaji kuzungumza na Yesu kwa yale yote yaliyowapata walipoenda mpaka waliporudi. Huu ndiyo wakati ambao Yohana mbatizaji alikuwa ameuwawa na Yesu kwa huzuni alitaka kuomboleza kifo cha mtu wa karibu Kwake akiwa mahali penye utulivu. Hata mitume walihitaji penye utulivu, pasipo na wapelelezi na fujo fujo za watu au mashutumu ya Mafarisayo. Yesu hataki tufanye kazi bila kupumzika au kutafakari kinachofanyika na kupanga kukifanya kwa ufanisi. Hata leo kupumzika ni jambo la muhimu sana. Kwa wote wanaohudumia watu ili Shetani asituingie tukiwa tumechoka na udhaifu hata tukose muda wa kuhusiana na Mungu wetu. Ni uwezo wa Mungu ndiyo unaotufanya tufanye kazi Yake kwa ufanisi. Lazima tuchukue muda kusoma Maandiko, kuomba na kutafakari ili tuunganishwe Naye kwa mahusiano mema yenye upendo.

*MUNGU Anajibu Maombi ya Imani Kwa Nguvu —Wakati watu wanajitoa kama Eliya na wanamiliki imani aliyokuwa nayo, MUNGU atajifunua kama alivyofanya wakati huo. Watu watakapokuwa wanamsihi Bwana kama vile Yakobo, majibu/ matokeo ambayo yalionekana wakati huo yataonekana tena. Nguvu zitatoka kwa MUNGU kujibu maombi ya imani.
---------------------------------

Maswali: Kuna tofauti gani kati ya mitume 70 na mitume 12? Mbwa mwitu ni nani na kondoo ni nani duniani leo? Yesu aliwaambia wanafunzi wafurahi kwa ajili gani? Yesu aliwapa wanafunzi mamlaka gani?

**SIKU YA 227.**
**(Agosti 14)**

# Msamaria mwema mwenye huruma.

**Luka 10.**



Mitume walikuwa wamebarikiwa sana kwani wengi walitaka kuyaona aliyoyafanya Yesu kwa macho yao. Mfalme Daudi, Ibrahimu na wengine wangeruka ruka kumwona Masihi. Hata wengi walioonekana wenye hekima walifichwa vingi bali wao walielezwa kila kitu, nasi tuna bahati leo kuwa na Neno la Mungu maaana yale waliyoelezwa mitume tunayo. Basi hata sisi leo tuna nafasi ya kufanya kazi kwa wale wenye mahitaji, iwe ni shuleni kwetu, kwa wazazi wetu, ndugu zetu marafiki zetu na hata kwa yoyote mwenye mahitaji kama Msamaria mwema tunayeenda kusoma habari Zake.

Ni rahisi kusimulia kisa cha wokovu kwa watu kwa kuweka mfano mzuri wa kujali watu na kuwa na huruma. Upendo ndiyo msingi wa ufalme wa mbinguni; kumpenda Mungu wetu wa mbinguni na jirani zetu. Toka utoto tumefundishwa kujifikiria na kujipigania kwanza ndiyo tukumbuke wengine; bali ufalme wa Yesu wasema tuangalie mahitaji ya wengine. Kwenye ufalme wa Mungu, ukipigana vita mwenyewe bila kumtegemea Mungu, unashindwa, bali ukijisalimisha Kwake unashinda vita. Saa ile ile waliporudi mitume wale 70, Yesu alishangilia kwa Roho Mtakatifu akisema "Nakushukuru Baba, BWANA wa mbingu na nchi kwa kuwa mambo haya umewaficha wenye hekima na akili; umewafunulia watoto wachanga; Naam baba kwa kuwa ndivyo ilivyokupendeza."

Akawaambia amekabidhiwa vyote na BABA "Yake na wala hakuna amjuaye Mwana ila Baba; wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana na Ye yote ambaye Mwana apenda kumfunulia." Akawageukia wanafunzi kwa faragha akawaambia wana baraka sana kwamba wanaona yale mambo, maana manabii wengi na wafalme walitamani kuyaona yale wasiyaone wala kusikia yale mitume waliyoyaona. Kweli mitume walikuwa na bahati iliyoje kusimama uso kwa uso na BWANA Yesu mwenyewe, Je nawe usingependa kupata nafasi hiyo?

Na tazama akaja mwanasheria mmoja akasimama karibu naye akisema, mwalimu "nifanyaje ili niurithi uzima wa milele." Yesu akijua alikuwa akitaka majadiliano au mabishano, alimjibu kwa swali, akamwambia imeandikwa nini katika torati, wewe unaisomaje? Akajibu vizuri, muhtasari ya sheria yote "Mpende BWANA Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote na kwa akili zako zote na jirani yako kama nafsi yako'. Yesu akamwambia yuko sawa kabisa basi "fanya hivyo nawe ili uishi." Akitaka kujidai ana haki japo alikosa maneno maana alitaka kuwa sawa na kunuia kuepuka jukumu la kumpenda jirani maana waandishi walikuwa watu wanafiki wanaojipenda, wakijionyesha mbele ya watu kwamba ni watu wa dini, ila mioyoni mwao yao walikuwa hawapendi watu au Mungu alisema "jirani yangu ni nani?'
Ndipo Yesu akasema mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia mkononi mwa majambazi, nao wakamvua nguo zake, na kumjeruhi, kisha wakenda zao wakimwacha mahututi karibia kufa. Kwa bahati nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile na alipomwona alipita kando. Na Mlawi vivyo hivyo. Lakini Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo na alipomwona alimhurumia, akakaribia akaosha na kufunga vidonda vyake, akivitia dawa ya mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake. Akampeleka nyumba ya wageni, akamtunza. Hata siku ya pili akatoa pesa dinari mbili, na kumpa mwenye nyumba ya wageni akimwambia "mtunze huyu mgonjwa niliyemleta, na chochote utakachogarimiwa zaidi, mimi nikaporudi kutoka safari yangu nitakulipa.

Yesu akamalizia kisa kwa kumwuliza yule mwanasheria "ni yupi kati yao watatu aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya majambazi?" Yule mwanasheria akajibu, ni yule aliyemwonea huruma. Yesu akamwambia aende zake, naye akafanye vivyo hivyo. Yesu alijibu swali kwa sisi binadamu wote. Hata leo hivi, jirani zetu si ndugu zetu tu, au watu wa kabila moja na sisi tu, au wanaoishi karibu na sisi, au watu wa madhehebu yetu tu, au marafiki zetu tu. Jirani zetu ni wale wote wanaohitaji msaada wetu. Yesu alimaliza kabisa maswali yetu ya 'nani ni jirani yangu' hata leo. Torati ya Musa ilieleza kuwa na fadhila na rehema kwa yatima, wajane, wageni, watu baki tusiowajua na masikini.

Msamaria alikuwa anajitia hatarini, kusimama kwenye barabara iliyojulikana kwa majambazi, na kufanya kazi ya kutoa jasho kwa kumbeba mtu na kumweka kwenye punda wake? Kuwa na huruma na kusaidia wenye mahitaji, bila kujifikiria mwenyewe ni muhimu sana. Usiseme kwamba sasa ni saa yako ya kupumzika "usinibughudhi, usinisumbue sina deni lako", hiyo ni kukiuka kanuni za mbinguni. Wengine husema sitamsaidia mtu hapa hospitalini. Pengine manesi ni wachache, au wengine hawana huruma kumjali mgonjwa. Hayo yasikupe shida, wewe saidia pale inapowezekana na Mungu atakupa nafasi na baraka ya kutimiza shauku yako ya kusaidia watu. Yeye mwenyewe atakubeba na kukuwezesha.

Mara zingine mtu amejitia shidani mwenyewe, na kisha ukakataa kumsaidia anapopata shida. Pengine alipanda mti akicheza na kuanguka akavunjika, usiseme "amejitakia, anapata mshahara wake!" Maisha ya kupenda watu na kumpenda Mungu ndiyo siri ya ufalme wa mbinguni. Mungu ni Upendo. Siyo Mungu ana upendo la! Mungu ni Upendo wenyewe! Wengi wa mataifa mbali mbali kama alivyokuwa

Msamaria, hawajafikiwa na ujumbe na hawana Maandiko, bali wamekuwa wakipenda kanuni  za ufalme wa Mungu. Kwa mvuto wa Roho Mtakatifu, hawa wamekuwa mibaraka kwa wenzao. Watu hawa wamekuwa wakimwabudu Mungu bila kujua, kwani Roho amegusa maisha yao; nao wamekuwa vyombo vyake. Hawa ni watoto wa Mungu pia japo ni 'Wasamaria' au kwa lugha ya leo, japo hawamjui Mungu au Yesu Kristo kama sisi.

Mtu mwingine pia aliuliza swali hili, kwamba amri kuu ni zipi, bila nia ya kumweka mtegoni Yesu. Huyu alipojibiwa, Yesu alimwambia "hayupo mbali na ufalme wa Mungu." Basi kutembea katika nyayo Zake Yesu, si kwenda kuhiji Israeli au Misri, bali kufuata nyayo Zake katika kuwasaidia wale wenye shida na mahitaji, kihali na mali. Mfano kuna wapweke, wazee, yatima, wajane, watoto walioachwa kwenye mitaa, ushauri wa kitaaluma, wamishonari wa tiba n.k.

*Kwa ajili ya msamaha wa dhambi, kwa ajili ya Roho Mtakatifu, kwa ajili ya tabia kama ya Kristo, kwa ajili ya hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa ajili ya zawadi yoyote ambayo Ameiahidi, tunaweza kuomba; basi tunapaswa kuamini kwamba tunapokea, na kurudisha shukrani kwa MUNGU kwamba tumepokea
--------------------------

Maswali: Kwa nini wale waliomwona Yesu na kusikia mafundisho Yake wana baraka sana? Ni Jambo gani Jema Msamaria alilolifanya? Jirani yangu ni nani? Je kwa nini ni rahisi kusaidia marafiki, ndugu au watu wa kabila letu tu? Sisi ambao hatukumwona Yesu uso kwa uso alipokuja mara ya kwanza tuna baraka gani?

**SIKU YA 228.**
**(Agosti 15)**

# Mungu anatuhimiza tuutafute ufalme Wake na haki Yake kwanza.

**Mathayo 10.**

**Ninyi ni bora kuliko ndege hata wasioonekana wazuri.**
**Mathayo 10: 11.**

Yesu akawaambia wanafunzi Wake kwamba mashomoro wawili huuzwa kwa senti moja tu, ila hawaanguki au kufa bila Baba wa mbinguni kujua japo wana rangi isiyovutia ya kijivu na kahawia ukilinganisha na ndege wengine! Basi hata sisi binadamu, Mungu anatupenda mno, na hata nywele za vichwa vyetu zote zimehesabiwa. Si rahisi kujua namba za nywele za mtu. Wengine siku hizi huhesabu nywele zao pengine kwa kutumia mashine wakafika laki tatu mpaka laki tano kwenye kichwa kimoja. Mungu anatujali na kutupenda, anajua kila kitu kuhusu sisi. Anatujua kuliko sisi tunavyojijua wenyewe! Tusiogope maana tu bora kuliko mashomoro wengi. Basi tukimkiri Yeye mbele ya watu, Naye atatukiri mbele ya Baba Yake aliye mbinguni. Ila tukimkana, na kusema hatumjui mbele ya watu, Naye atatukana mbele za Baba Yake wa mbinguni. Na tunapokosea kwa kumkana kama Mwanamatengenezo Jerome, tuombe msamaha na kuanza safari mpya ya matumaini. Mungu anakubali moyo uliopondeka na wa toba.

Akaendelea kuwaambia, wasidhani kwamba alikuja kuleta amani duniani, bali upanga na vita. Alikuja kuleta ugomvi na fitina kati ya mtu na babaye, binti na mamaye na mkwe na mkwe mtu. Maana mmoja kati yao akimwamini Mungu, mwingine atachukia na kumfanyia vituko mwenzake. Adui wa mtu ni wale wa nyumbani mwake. Yule mtu anayependa baba au mama kuliko Mungu, hamstahili, Yeye, au apendaye mwana au binti kuliko Mungu hamstahili Mungu. Yule anayejaribu kuokoa nafsi yake ataipoteza naye mwenye kuipoteza nafsi yake kwa ajili ya Kristo ataipata.

Yesu alijua waumini watachukiwa kama Yeye alivyochukiwa na watu. Watu wengine walimchukia wakiona watu waja Kwake na anawasikiliza na kuwasaidia katika shida zao. Hata leo mambo ya namna hii yanatokea, endapo mpo shuleni na unajitahidi kuwa mtii na kuwa na adabu njema waweza kuchukiwa. Ukijitahidi ujisomee na kupata maksi nzuri, kuna watoto watakaokuchukia, kwamba unajipendekeza. Katika kufundisha nimekutana na watoto wanaojifelisha au kufanya jambo la uovu kama kukosa adabu ili wafanane na wengine. Wale waliomchukia Yesu walijaribu kumweka kwenye shida au kona au hatari, ila wale walipompenda hawakufuata watu wengine waovu, bali walikuwa tayari kufanya mema kwa Yesu.

Yoyote ampokeaye mtu wa Mungu atakuwa amempokea Mungu na Yesu. Naye ampokeaye nabii kwa kuwa ni nabii, atapata thawabu au baraka ya nabii. Naye ampokeaye mwenye haki, atapata thawabu ya mwenye haki. Pia yoyote atakayempa yoyote mdogo au mdhaifu hata maji ya baridi tu kwenye kikombe kwa kuwa ni mwanafunzi, amini haitapotea kamwe thawabu yake.

Yesu alisikitika alipoona miji fulani aliyokuwa amefanya miujiza mikubwa watu wakikataa kuungama dhambi zao na kupata toba ya kweli. Kwa maana alijua yaliyo ndani ya mioyo ya mwanadamu, hata wakisema kwa unafiki, aliweza kuisoma mioyo yao zaidi ya walivyojijua wenyewe. Naye Akasema "Ole wako Korazini, Ole wako Bethsaida, Ole Kapernaumu akimaanisha, nawahurumia Korazini, Bethsaida na Kapernaumu" maana wamepata nafasi kuliko wengine ya kuhubiriwa nao hawakufanya maamuzi ya kumwamini Mungu au kuachana na dini ya mapokeo. Akasema ikiwa kama ile miujiza aliyoifanya miji hiyo ingelifanywa kwa mataifa kama Tiro na Sidoni wangelitubu zamani kwa kuvaa magunia na kujipaka majivu kuonyesha kujuta na huzuni yao.

Akasema itakuwa rahisi kwa Tiro na Sidoni kustahimili hukumu maana hawakujaliwa kujua mengi kuliko wao waliojua mengi ila wasiyafanye. Akasema Sodoma na Gomora ingetendewa miujiza hii yote, ingesalimika hata leo wala isingechomwa. Akasema itakuwa rahisi kwa nchi ya Sodoma kustahimili adhabu yake siku ya hukumu kuliko wale waliopata nafasi ya kufundishwa Neno la Mungu na wasilisome au wasilitende. Mtu aliyepewa vingi huwiwa vingi. Hata leo sisi tuliopewa Maandiko tumepata vingi, hivyo tumwombe Mungu tuyasome na kuyatekeleza.

Mafarisayo na Masadukayo waliokuwa na uadui, walianza kupatana. Kwa vile walikuwa na adui mmoja, Naye ni Yesu, hicho kilifanya wawe marafiki. Hata leo tuepuke hilo, yaani walifanya adui wa adui yao kuwa rafiki yao. Tuwapende wale tunaodhani ni maadui zetu hata wale tunaowaona kama kwamba hawapendeki, hao nao tuwapende.

Mafundisho ya Yesu yalionekana kupinga mapokeo ya viongozi wa kanisa wa siku zile, kwa vile hakufundisha mapokeo, desturi au sheria zao. Maisha yake yaliwashitaki wakajiona wanapoteza hadhi na heshima zao kama viongozi wa kanisa au wa kiroho. Maisha yao yalikuwa na uovu na alitaka awasaidie viongozi na raia wa kawaida waliojiita ni waumini. Alijua serikali ya Kirumi ina ukatili, na kunyanyasa, ila hakusumbuka kwenda kuzibadilisha serikali za dunia, bali watu walio makanisani au waumini waliotangaza kwamba wao wanamwamini Mungu na kumtumikia, na kisha wakaenda kinyume cha tabia ya Mungu.

Roho Mtakatifu aligusa watu na ile Kweli ya Neno, ila walikuwa na uchaguzi wa kukataa au kukubali. Yesu aliyeweza kuponya kila aina ya ugonjwa, kufufua wafu na kufundisha mafundisho ya kushangaza, ila hakuweza kufikia mioyo ya watu walioweka mapazia, kwani walikuwa kama vipofu katika uchaguzi wao na chuki na ubaguzi vikawajaa. Kubadilika kwa moyo ni muujiza mkubwa sana, ila Yesu hawezi kutulazimisha; bali tukimkubalia atufanyie muujiza huu, atakuwa na furaha sana kuufanya. Kama tumepata elimu na hekima ya kuweza kulipata Neno Lake kwa

kuambiwa na watu au kulinunua, tuna jukumu la kulifuata bila kusita na kujiepusha kusema kesho! Kesho! ndiyo nitatii Neno la Mungu.

Twahitaji pia kuomba, na kufunga, ili tupewe imani inayofanana na hata punje ya Haradali. Punje hii ilikuwa ndogo kupita zote zilizopandwa enzi zile. Zamani zile kitu kidogo cha namna ile tulisema 'kinong'oningo' yaani kidogo sana. Hebu tumpe Mungu utukufu kwa kila jambo; mawazo, nia, maneno na hata matendo, maana yote tuyafanyayo ni Yeye anayetuwezesha kuyafanya.

*Kuishi kwa Neno la MUNGU kunamaanisha kusalimisha Kwake maisha yote. Kutakuwa na hisia ya kuendelea kuwa na uhitaji na utegemezi, kuuvuta moyo kumfuata MUNGU. Maombi ni lazima; kwani ni uhai wa roho. Maombi ya familia, maombi ya hadhara, yana nafasi yake; lakini ni ushirika wa siri na MUNGU ndiyo unaodumisha maisha ya roho.
---------------------------------

Maswali: Sisi ni bora kuliko ndege gani? Nywele zetu zimehesabiwa ina maana gani? Kwa nini Tiro na Sidoni walipewa sifa kulinganisha Kapernaumu, Bethsaida na Korazini? Kwa nini waovu wanachukia watu wema? Utajuaje tofauti ya mtu anayechukiwa kwa wema wake au kwa uovu wake?

**SIKU YA 229**
**(Agosti 16)**

**KUBEBA MSALABA**

# Gharama ya kuwa mwanafunzi wa Yesu.

**Luka 12,14 na Mathayo 10.**



Yesu aliwaambia wanafunzi Wake kuna gharama ya kuwa mfuasi Wake. Mtu yoyote anayetaka kumfuata sharti, abebe msalaba wake na amfuate, katika kushiriki dhiki Zake. Katika historia ya kanisa watu wamejitoa mhanga kimali na hata kihali. Wengine wamewekwa magerezani, wameteswa miili yao, wamefukuzwa kazi, wamechekwa, wamefukuzwa na jamaa zao, au hata kuuwawa kwa ajili ya Kristo. Ni Mungu tu anayejua watu Wake wamepata shida kwa kiasi gani.

Watu wengi siku hizi wanahubiri injili ya mafanikio ya mali, injili ya utajirisho. Kwamba wote wanaomwamini Mungu wataishi raha mstarehe na utajiri mwingi. (Prosperity gospel au injili ya utajirisho) Hawa wanaahidi watu kwamba kwa kumfuata Yesu na kutoa sadaka kwenye huduma fulani, watakuwa na magari, pesa, majumba na mambo yote ya fahari. Wachungaji wengine wa nchi fulani wamekuwa mabilionea na kununua ndege za gharama na kuruka kwenda huku na kule, na pengine hata kuwa wabaradhifu wa sadaka za washiriki, hawa hawatendi vile Masihi anataka! Cha kuelewa ni kwamba wengi hawatakuwa matajiri katika dunia hii, hata wale wanaomwamini Mungu; ila mwishowe Yesu atatupa zawadi za thamani zaidi ya mali. Tutaona mbingu ilikuwa rahisi sana kuipata, na kwamba hatukujinyima vya kutosha kustahili kuingia pale ukilinganisha na ule uzuri Wake.

Yesu alisema alikuja kuleta moto, na mafarakano; baba atagombana na watoto, mabinti watagombana na mama zao, na mkamwana atagombana na mama mkwe wake. Akasema yeyote anayekuja Kwake bila kumchukia, babaye, mamaye, mtoto wake, dada, kaka au yeye binafsi; hawezi kuwa mwanafunzi Wake. Yeye ampendaye baba, mama, rafiki, au yeyote kuzidi Yesu hamstahili Yesu. Yeye asiyechukua msalaba wake na kumfuata, hamstahili. Yeye anayetaka kutunza maisha yake atayapoteza

na atakayepoteza, atayatunza. Yesu alimaanisha kwamba chochote tunachokipenda kuzidi Yeye, basi hatumstahili. Hii ni pamoja na kujipenda wenyewe, kupenda marafiki, ndugu, familia au kitu chochote. Yeye apaswa kuwa namba moja katika maisha yetu.

Kuwa mwanafunzi na mfuasi wa Yesu ni kumkubali Yeye kama Kristo, Mwokozi na BWANA wa maisha yetu. Twapasa Kumfuata Yeye kama namba moja kisha vingine ndiyo vifuate. Kumkubali Yesu ni pamoja na kujua mateso yaweza kutokea ila tusiogope kutoa ujumbe kamili kwa kuogopa mateso. Kuwa mfuasi wa Yesu, kwahitaji nidhamu. Watu wengine waliona kwamba mbona Yesu anataka kumiliki maisha yao? Ukweli ni kwamba, hatuwezi kufanya tunavyopenda na kuwa Wakristo au watu wa Mungu. Tuko shule ya Kristo ili tabia zetu zifanane Naye. Tabia tu ndiyo kitu tutabeba kwenda nacho mbinguni, lakini vingine vyote tutaacha, hivyo tabia yapaswa ijengewe na kujengeka ili kufanana Naye.
Yesu aliwambia mitume lazima aende Yerusalemu na atateswa na wazee, makuhani na waandishi kisha atauwawa. Petro akakanusha, haya yasimtokee. Yesu akasema "Ondoka nyuma Yangu Shetani kwa maana huyawazi yaliyo moyoni mwa Mungu." Mioyo yetu ni midanganyifu na hakika ukiangalia ni masaa machache tu Petro alikuwa amemkiri Yesu kuwa Masihi na Mwana wa Mungu aliye hai. Haukupita muda, akawa kama Shetani. Mtu asione amesimama kwa uwezo wake, maana ndipo ataanguka kirahisi.

Yesu aliwaambia watu watawafukuza kwenye makanisa, wasiwe washiriki na wengine watawaua wakifikiri wanamfanyia Mungu kazi. Hili jambo limetimia kwani kumezuka watu leo wanaoua wengine wasio na makosa, wakifikiri wanafanya mapenzi ya Mungu au Mungu amewaagiza. Yesu akawatahadharisha, ulimwengu ukiwafanyia ubaya huu wakumbuke hata Yesu walimfanyia vile. Ulimwengu hupenda watu waliowaovu, ila watu wanaompenda Mungu wanapewa mateso na watu wa dunia. Kabla ya kumfuata Yesu ni muhimu kuhesabu gharama. Ila hakuna kitu ambacho dunia inakitoa kilicho cha thamani kuliko kile Yesu anachotoa.
Kila ndoto, njozi, mawazo, na matakwa lazima yawekwe chini ya nira ya Yesu. Kila talanta, uwezo, mali, au chochote cha thamani lazima kisalimishwe kwa Yesu; la sivyo kitu hicho kitakuwa Mungu, na kutupotezea malengo. Hii ni ikiwemo nadharia na maoni yetu wenyewe! Wanariadha kabla ya mashindano, wanafanya mazoezi kwa bidii, pengine hata siku nzima, wakila chakula cha aina fulani tu, na kuwa na nidhamu za kunywa maji, kulala masaa fulani, na mengineyo, ili kusudi washinde. Huacha anasa, na burudani zote, na kuweka matakwa yote nyuma. Hakuna anayewalazimisha kufanya mazoezi hayo, ila wananuia ili wapate medali. Je, mkristo haimpasi kuwa makini zaidi ya hayo? Thawabu za wanamichezo au mambo ya dunia ni vya muda mfupi, ila zawadi ya kupiga mbio zihusuzo kuingia mbinguni ni za milele.

Mtu kabla ya kujenga jengo, lazima afanye mahesabu, asije kuchekwa ameshindwa kumaliza jengo. Hata kabla ya kwenda vitani, nchi lazima ijipime kama inaweza kupigana na mtu yule, kama haiwezi, itabidi kutuma ujumbe wa mapatano, la sivyo watapigwa na kuumizwa. Kuhesabu gharama za kuwa mfuasi ni pamoja na gharama za kuumizwa kwa hisia, kukataliwa na jamii, kuwa masikini, kuwekwa

jela na hata kuuwawa. Mkono wa mtu au mguu ukimkosesha ni vyema aukate, na kuutupa; ni bora kuingia uzima wa milele kwa kupungukiwa mkono au mguu, kuliko kwenda Jehanamu na viungo vyote. Jicho likikukosesha basi inabidi kungoa, ni bora kuingia mbinguni chongo kuliko kutupwa Jehanamu.

Twapaswa kuwapenda maadui wetu, kuwatendea mema na kuwawakopesha bila kutoa riba, na thawabu yetu itakuwa nyingi. Mtu yoyote aliyeacha nyumba, mke, ndugu, wazazi, au wana kwa ajili ya ufalme wa Mungu atapokea mara nyingi zaidi, katika ulimwengu huu na zaidi katika ulimwengu ujao uzima wa milele. Wanafunzi wanapaswa wasifadhaike, maana Yesu amewaandalia makao, ili pale alipo nao wawepo. Katika Waebrania 11, sura ya 'watu wenye imani' tunaona wengi waliopiga mbio na shida walizozipata. Wengi waliteswa, ila watafufuka katika ufufuo wa kwanza; ufufuo ule bora.
Tukimfuata Yesu lazima tubebe msalaba. Kila mkristo ana msalaba, mkristo lazima aachane na anasa na yote ya dunia. Msiipende dunia wala mambo yaliyomo.

Tunaweza kuzungumza na MUNGU mioyoni mwetu; tunaweza kutembea katika ushirika na Kristo. Tunapofanya kazi zetu za kila siku, tunaweza kuleta matamanio ya mioyo yetu, shauku isiyoweza kusikiwa na sikio la mwanadamu; lakini neno hilo haliwezi kufa kimya, wala haliwezi kupotea. Hakuna kitu kinachoweza kuzamisha shauku ya roho. Kwani hii huinuka juu ya sauti za mitaani, juu ya kelele za mashine. Ni MUNGU Ndiye ambaye tunazungumza Naye, na maombi yetu husikilizwa.
-------------------------

Maswali: Kubeba msalaba wetu ina maana gani? Kwa nini mtu akijenga au akienda vitani sharti akae na kupiga mahesabu? Kwa nini apendaye baba, mama au ndugu kuliko Yesu hamstahili?

**SIKU YA 230.**
**(Agosti 17)**

# Ufalme wa mbinguni ni Lulu ya thamani, au nyavu ya samaki.

**Mathayo 13.**



Yesu aliendelea kuzungumza kwa mifano, hii ilileta umakini wa usikilizaji, na kupembua. Ilifanya wabaguzi wa Yesu wasilete taabu kwa wale waliokuwa tayari kusikiliza. Baadaye alipokufa na kufufuka wengi walikumbuka mifano Yake na mawazo yao yakawa tayari kutumiwa na Roho wa Mungu ili wabadilike. Hata leo, wengi wanaendelea kuvuviwa kutoa tafsiri nzuri za mifano hii, na kuieleza kwa namna nyingi tofauti tofauti kwa kuvuvia wengi kwa Yesu. Yesu akasema ufalme wa Mungu umefanana na mfanya biashara mwenye kutafuta lulu nzuri, naye alipoona lulu moja ya thamani kubwa alikwenda akauza vyote alivyo navyo ili ainunue. Wala hakutaka kuchuuza, yaani kumwambia yule mwenye lulu apunguze bei, maana alijua ni kitu cha thamani kubwa.

Hata leo tusiangalie ni machache kiasi gani twaweza kuyafanya na bado tufike mbinguni. Kuna wimbo watoto waliimba darasa la kwanza ulisema “Mkulima

mwenye shamba, alipanda viazi, akachimba chimba akaona almasi, lo! lo! bahati, ya mtu mwenye shamba. Akatupa Jembe upande, akaenda zake mjini, kununua gari lake, sasa ni tajiri. Lo! lo! Bahati ya mtu mwenye shamba." Ufalme wa Mbinguni ni kitu cha thamani mno. Inabidi tuweke vyote kando na kuutatufa huo, maana kila kitu chema tutakipata kule, ila vya dunia vinatokomea, na vingine havileti furaha kabisa. Hivyo yabidi tutafute ufalme wa Mungu kwanza na haki Yake, na vile vingine Mungu atatupa kama bonasi.

Yesu ndiyo Lulu ile ya thamani, hebu tuitafute leo. Lulu inatengenezwa kwa njia za ajabu, pia ina bei kubwa. Konokono wa baharini ndiyo hutengeneza hiyo lulu wakati punje ya mchanga ikiingia kwenye nyumba yao. Lulu inaanza kuumbika kuzunguka hiyo punje ya mchanga. Lulu inapendeza kwa macho na kung'aa, na wengi hupenda kuiangalia kwa masaa. Mara nyingi huwa na ukubwa wa njegere, ila kuna zingine chache ambazo ni kubwa zaidi. Thamani ya lulu mara zingine hushinda thamani ya dhahabu. Wazamia maji baharini hutafuta konokono au kaa hawa (oysters?) na mara nyingi hawapati kitu ila wakipata hutafuta pa kuuza. Hupata bei nzuri kwa vile lulu yapendeza na ni adimu kupatikana. Yoyote anayeanza mahusiano yake na Mungu, na kumtii atakuwa amegundua Lulu ya thamani kupita zote.

Kisha akatoa mfano mwingine akisema ufalme wa mbinguni umefanana na nyavu iliyotupwa baharini na kukusanya samaki, kaa, majani, na takataka zingine. Watu walipolivuta jarife hili pwani walichukua samaki wale wazuri, na vile vingine visivyofaa walivitupa. Ndiyo itakavyokuwa mwisho wa dunia, malaika watatokea na kutenga waovu mbali na wenye haki mbali. Waovu watatupwa kwenye tanuru la moto, ndipo watalia kilio kikuu cha uchungu na kusaga meno. Wengi wamejiuliza mbona kuna watu waovu ila wanalitaja Jina la Mungu na kwenda kwenye ibada? Biblia imeweka wazi hili kwa kusema; si kila mtu amwitaye Yesu BWANA ataingia mbinguni, bali alifuataye Neno Lake.

Akasema wengine siku ya mwisho watasema walifanya miujiza kwa Jina Lake, mbona hawajaingizwa mbinguni. Naye atasema sikuwajua. Maana ya Mungu kutujua ni nini? Si kutojua kama vile ametuumba, bali ni kutojua kwamba tumejua Neno lake na kujitoa kikamilifu, tukiishi kwalo. Waingereza wanasema kusalimu amri, au kujisalimisha. Ni kuyafia maisha yetu ya zamani, tukiacha vyote vya ubinafsi na kujifikiria ili Yesu aishi katika maisha yetu mapya. Kitu kikubwa mtoto au mtu mzima anachohitaji ni kutoangalia wengine, bali kukaza nia kwani tumo katika shindano kubwa kupita yote. Yesu akauliza kama wameyafahamu haya? Kisha akasema "Kila mwandishi wa sheria mwenye elimu ya ufalme wa mbinguni amefanana na mtu mwenye nyumba atoaye katika hazina yake vitu vipya na vya kale. Akimaanisha kwamba sote tunaompenda Mungu tunaweza kuyapa mafundisho ya zamani uzuri yakaonekana ya thamani na ya ajabu kabisa.

Yesu anatupenda mno, alimtuma Mwana wake wa pekee aishi na kutoa mafundisho, ili watu wayasikie na kuyatii. Yesu hakufundisha mashuleni ila alifundisha pale watu walipokutanika, kama vile kwenye mlima wa baraka, au pwani. Alitumia mifano na visa vya kawaida, ambavyo vilieleweka. Mifano hii ilisaidia watu kuelewa ujumbe aliotaka wapate, na ikawa rahisi kuwasimulia wengine pia. Je unafikiri Yesu angekuwa

nasi leo mjini mwetu angekaa wapi afundishe? Je angetoa mifano gani? Pengine angetoa mifano ya simu za mkononi, redio, ndoo za plastiki, au ndege na mabasi yanayopita? Hivi havikuwepo siku zile. Yesu alifundisha mambo muhimu kupita yote duniani. Alizungumzia upendo wa Mungu kwa mifano rahisi. Alizungumzia ufalme wake na uzima wa milele. Alifundisha Neno la Mungu, maombi na mahusiano yetu na Yeye na wenzetu. Yatupasa tusikilize kwa makini mafundisho ya Yesu. Yale anayotuambia ni muhimu kupita yale yote ambayo tunayasikia au kujifunza katika maisha yetu yote.

Yesu aliwafundisha watu kuhusu Yeye pia, akisema Yeye ni mkate wa uzima, Mchungaji mwema, na Mzabibu wa Kweli. Yesu ana majina mengi, zaidi ya mia tatu tunayoyajua, Soma kitabu kinachoitwa Jina Lipitalo Majina yote, humo kuna majina 365 ya Yesu na mengine tutayasikia tutakapofika mbinguni. Mara nyingi Yeye alizungumza wazi wazi, akisema anatoka kwa Mungu, na Baba Yake ni Mungu. Alisema Yeye ni njia ya Kweli ya kwenda kwa BABA au Mungu. Yesu ni Njia, Kweli na Uzima. Mafundisho yake yapaswa kushikwa; nayo yatatufanya tuwe huru. Mafundisho Yake ni msingi wa yote mema duniani. Tukijenga maisha yetu kwa hayo tutakuwa wenye hekima. Kama tukimpenda yatupasa tufanye yale ambayo anatuagiza na kumtii. Mungu yu karibu sana nasi. Yesu alisema uzima wa milele uko katika kumjua Yeye, maana Ndiye anayetoa thawabu ya uzima wa milele. Kila mtu anatafuta kuishi muda mrefu, bila kuzeeka, kuumwa magonjwa au kuwa na makunyanzi usoni.

Yesu Yupo tayari kusikia maombi yetu kwa kutupa uzima wa milele. Tukiomba na kusoma Neno Lake kila siku, tutasaidiwa kumkumbuka Mungu na kufuata njia Zake. Yesu Yu tayari kufanya vyote kwa ajili yetu ili tuokoke. Kwa kufa Kwake msalabani alijibu maswali ya kila malaika, na viumbe wa Mungu; swali la "Je Mungu anatupenda." Kila kiumbe kikagundua Mungu anatupenda Mno, na Yeye Mwenyewe ni Upendo, siyo ana Upendo bali ni Upendo!

*Ni jambo la ajabu kwamba tunaweza kuomba kwa ufanisi; kwamba wanadamu tusiostahili, tunaokosea tunayo nguvu ya kutoa maombi yetu kwa MUNGU. Je! Ni nguvu gani ya juu zaidi ambayo mwanadamu anaweza kutamani kuliko hii, - kuunganishwa na kuwasiliana na MUNGU asiye na ukomo? Mtu dhaifu, mwenye dhambi ana nafasi ya kuzungumza na Muumba Wake. Tunaweza kutamka maneno ambayo yanafika kwenye kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu. Tunaweza kuongea na Yesu tunapotembea njiani, Naye anasema, Mimi Niko mkono wako wa kuume.
------------------------------

Maswali: Twawezaje kutafuta ile Lulu ya thamani? Ufalme wa mbinguni umefananaje na nyavu ya samaki? Waovu watatengwa wapi na wema wataenda wapi? Orodhesha majina 10 mpaka 20 ya Yesu.

**SIKU YA 231.**
**(Agosti 18)**

# Mikate mitano, samaki wawili kulisha maelfu.

**Mathayo 14, Marko 6.**



Yesu hakujulikana kama mponyaji tu bali mfundishaji mzuri. Watu walipoyasikia mafundisho Yake, walisahau shida zao, na hata walio na njaa, njaa ilikoma wakaendelea kusikiliza kwa masaa mengi. Mafundisho Yake yalikuwa sumaku kwa watu. Alikuwa chemi chemi na mfereji wa yote mema. Yesu alizungumza kwa mifano ya kila siku, alipokaa kwenye mashua pwani akatoa mifano ya kusaidia roho za watu kwa hiyo. Watu waliikumbuka na kuishika mifano hiyo, na kuiona katika maisha yao. Alipowafundisha, hakuwambia majibu papo hapo, alitaka wao wenyewe wafikiri maana yake, kisha aliwawezesha kuelewa kwa ndani wale waliochagua ufalme wa Mungu.

Siku zile kufundisha kwa mifano, mithali na mafumbo kilikuwa kitu cha kawaida. Alitimiza pia unabii uliosema "Nitafumbua kinywa changu kwa mifano, nitayatamka yaliyositirika tangu awali." Watoto na watu wazima leo pia wanapenda masimulizi na visa kwenye mahubiri. Watu walipoenda zao, wanafunzi walimwuliza maana ya ile mifano. Naye akasema Yeye apandaye mbegu njema ni Mwana wa Adamu, yaani Emanueli (Mungu pamoja nasi). Shamba ni dunia, na mbegu njema ni wale

wanaoingia ufalme wa Mungu, na magugu ni watoto wa mwovu. Mpandaji magugu ni Ibilisi, wavunaji ni malaika, siku za mwisho waovu watakusanywa kwenda kwenye moto wa Jehanamu, hukutakuwa na kilio na kusaga meno. Ila watu wa Mungu watang'aa kama mwangaza wa jua, kwenye ufalme wa Baba wa mbinguni.

Watu walishangaaa mafundisho Yake na wakasema "huyu amepata wapi hekima hii na miujiza hii? Huyu si mwana wa seremala? Mamaye si aitwa Mariamu, na nduguze Yakobo, Simoni, Yusufu na Yuda, na dada zake wapo hapa kwetu. Huyu amepata wapi yote haya."Yesu aliwaambia "Nabii hakosi kupata heshima isipokuwa kwake mwenyewe. Cha kusikitisha ni kwamba hakufanya miujiza mingi kule kwao kwa sababu ya kutoamini kwao. Leo tuombe imani, maana kutokuamini kunafanya Mungu asifanye makuu maishani mwetu. Yesu alimwambia mzee Yairo "wewe amini tu!." Nawe usomapo leo "wewe amini tu", nami pia naamini. Kama una shida kuamini, mwombe Mungu imani. Ni mojawapo ya ahadi Zake, Naye atakuongezea imani.

Wakati huu ndipo Yesu alipopata habari za kifo cha Yohana mbatizaji, aliyemtayarisha njia na binamu upande wa mamaake. Alisikitika na akaenda na wanafunzi Wake ili awe peke yao faraghani; wakavuka kwa chombo. Ila makutano waliposikia walimfuata kwa kutembea kwa miguu wakafika walipokuwa wanaenda. Yesu alipoona makutano aliwahurumia kwa maana walikuwa kama kondoo asiye na mchungaji. Pengine viongozi wa kiroho wakati ule walikuwa si msaada. Makuhani wengi walikuwa masadukayo, na hii yenyewe, ilipunguza matumaini ya watu. Kwani masadukayo hawakuamini ya mbinguni au ufufuo. Mafundisho hayo yalikuwa ni ya kukatisha tamaa.

Basi Yesu akawaponya magonjwa yao na kuzungumza nao, hakupata nafasi ya kula wala kupumzika wakati mwingine. Ilipofika jioni, wanafunzi walimwambia saa zimekwisha "waage makutano waende vijijini mwao, maana hapa ni nyika tupu, wapate pa kula na kulala, saa imekwisha."Yesu akawaambia hawana haja ya kwenda "wapeni ninyi vyakula." Wanafunzi wakashangaa maana kulikuwa na maelfu ya watu. Filipo akasema ingetumika dinari 200 au maelfu ya dola kulisha watu hawa. Basi Yesu akauliza wana kitu gani? Hapo Andrea alimwona mtoto wa kiume mwenye mikate mitano na samaki wawili; akampa taarifa Yesu. Mtoto huyu huenda alikuwa amevua samaki, na mamaye akamtengenezea mikate midogo midogo, asubuhi akaamka aende kumsikiliza Yesu; kumbe akabariki wengi na chakula chake. Hata Yesu BWANA Mwenyewe alikula chakula chake. Hata nawe kidogo ulicho nacho, chaweza kumbariki Yesu na wengine.

Andrea hasemwi sana kama kaka yake Petro, ila alionekana akishughulika ili mambo yaende sawa. Yesu akawaambia wanafunzi wamletee mikate na wale samaki wa yule mtoto, kisha akawaambia makutano wakae kwenye majani safu za watu hamsini hamsini. Akatwaa wale samaki na mikate na kutazama mbinguni, akaibariki na kuimega ile mikate na kuwapa wanafunzi na wanafunzi nao wakawapa watu, wakala wakashiba na kusaza. Ndipo nao wakakaa wale. Wakazoa masazo ya vipande vya mikate na samaki vikapu kumi na mbili. Hii yatufundisha tusiharibu chakula kilichobaki, kwani kuna wengi masikini wanaojihitaji. Kama unajua hutamaliza

chakula basi usipakue zaidi kwenye sahani yako. Kula kile unachopakua tu na ukimaliza rudia tena kupakua kidogo na ukimalize.

Kama una chakula kingi, au mali nyingi usitupe tupe, na kuwa mharibifu, wape wenye mahitaji. Muujiza huu waonyesha kwamba Mungu Ndiye atupaye riziki au mahitaji yetu ya kila siku, na tukiwa tayari kugawia wengine, Yeye daima atahakikisha kwamba tunakuwa na riziki zetu, iwe ni malazi, mavazi au chakula. Yeye hulisha viumbe vyake vyote, iwe ndege wa angani na wanyama, Isitoshe binadamu ndiye mwenye thamani zaidi, atakosaje kulishwa. Hata tuwe na akili nyingi au uwezo wa namna gani tukumbuke kwamba tunawapa watu vile tu ambavyo Mungu anatupa, hatuwezi kutoa zaidi ya vile tulivyopokea. Hakuna mwenye uwezo wa kupata chochote chema mwenyewe. Ila jinsi tunavyowagawia wengine ndiyo jinsi tunavyobarikiwa.

Si haki kuachia kazi ya kugawa mikate kwa wachungaji au watenda kazi wa kanisa. Tunapolishwa Neno la Mungu, twapasa tuwagawie wengine ili tuzidi kubarikiwa zaidi na zaidi. Tunapotoa vitu vyetu kusaidia wengine kama huyu mtoto, tunapata furaha zaidi kuliko wao tukiona tumekuwa mfereji wa baraka. Watu na marafiki zake wakasema hivi ni nani alileta hii mikate? Akaona wengi wanamsonda kidole "Unaona hii mikate inatoka kwa rafiki yetu yuleee!" naye akapata tabasamu. Yesu japo ana uwezo wote, hakuwapa watu vyakula vya fahari. Watu walifurahia mlo huu wa kawaida kuliko wangepewa mapochopocho ya karamuni. Hata leo tukiishi maisha rahisi bila ya kujiingiza kwenye gharama za vyakula vyenye fahari na visivyo na afya, inatufanya tuingie mitegoni kwa kuwa wachoyo kusaidia wenye mahitaji au kuingia katika shida. Tukiwa na vitu vya kawaida ni rahisi kuvigawa.

Yesu alitumia muda Wake katika kila tendo kuwafundisha watu masomo fulani. Hapa Yesu anatufundisha kwamba mahitaji au riziki zetu zote ni Yeye anatupa kila siku. Hata leo Mungu anafanya miujiza hii kila siku, kwa kupanda mbegu hadi kuvuna, ni miujiza kupata chakula na kuweka mezani mwetu. Chakula kilichobaki pengine kila mtume alichukua kapu nyumbani na kugawia wengine. Baraka ile ikazidi kutawanyika. Tunapomfuata Mungu kwa uaminifu, tuwe na amani moyoni kwamba atatusaidia kila hitaji letu, basi tumwite kwa maombi. Endapo tuna shida, tumwambie Yeye. Wote waliokula siku ile walikuwa wanaume 5000, bila kuhesabu wanawake na watoto. Endapo hesabu ya wanaume ilikuwa hiyo, basi jumla ya walaji wote, yaani wanaume wanawake, na watoto ilikuwa watu wasiopungua 15,000 hivi. Watu walisema siku ile "hakika huyu ni nabii aujiaye ulimwengu." Basi alikuwa zaidi ya nabii, alikuwa Emanueli na Masihi!. Mtoto mdogo aliyekuwa na samaki na mikate, akawa mbaraka kwa kutumiwa na Yesu. Pengine Yesu akamshukuru yule mtoto kwa jina lake. Maisha ya mtoto huyu yalibadilika siku ile. Hata leo mtoto, usione kwamba huna karama kubwa au vitu vya maana. Ukiwa na vidogo na unyenyekevu alivyokupa Mwenyezi Mungu, huwa vikubwa. Hata mkiwa na wageni kwenu, na chakula kisitoshe mwombe Mungu na atakizidisha. Utashangaa kila mtu atakaposhiba na kikabaki, kwa vile umetoa kwa moyo wako.
Ukitaka kusaidia wenye mahitaji utabarikiwa na hata wewe utatimiziwa mahitaji yako na zaidi ya yote utakuwa na furaha ya ajabu kutoka Kwake.

*Yesu Anatualika Kuomba— Bwana anatupatia fursa ya kumtafuta Yeye binafsi katika maombi ya bidii, ya kutua mizigo ya roho zetu Kwake, bila kumficha chochote Yeye ambaye ametualika, “Njooni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo. Nami nitawapumzisha. ” Oh, tunapaswa kushukuru sana kwamba Yesu Yuko tayari na ana uwezo wa kubeba madhaifu yetu yote na kututia nguvu na kuponya magonjwa yetu yote ikiwa itakuwa kwa faida yetu na kwa utukufu Wake.


------------------------------

Maswali: Ibilisi anapandaje magugu leo? Kwa nini mbinguni hakuna magugu? Wewe unawezaje kumkataza Ibilisi asipande magugu? Kwa nini Yesu hakufanya miujiza mingi kwao? Kwa nini Yesu alisema wale watu wakae mafungu ya watu hamsini hamsini? Kwa nini ni muhimu kuwalisha watu wenye njaa?

**SIKU YA 232.**
**( Agosti 19)**

# Petro atembea juu ya maji.

**Marko 6.**



Baada ya kuwalisha mikate, Yesu alitambua watu walitaka kumkamata na kumfanya awe mfalme, kwa vile walipata chakula. Waliona mfalme huyu mwenye chakula kingi atasaidia matumbo yao yasiungurume kwa njaa. Watu hawa pia walitaka mtu mwenye uwezo wa kuwatoa kwenye milki ya Warumi. Yesu hakuwa kiongozi wa siasa, bali wa kiroho. Hata mtu aliyependa kuwa kiongozi kwa watu hawa alikuwa na kazi maana walikuwa vigeugeu, mara moja wanahamaki na kuchukia, dakika inayofuata wana upendo na furaha tele. Wanafunzi nao walikuwa wamechoka kubeba mamia au maelfu ya vikapu vya mikate.

Yesuakajitengaakaendamlimaniawe peke Yake aombe; akawalazimisha wanafunzi wake kutangulia mbele Yake kwenda ng'ambo wakati Yeye akiaga makutano. Kisha akajitenga faragha mlimani awe peke yake aombe, na kulipokuwa jioni akiwa peke Yake, chombo na mitume kilikuwa kimefika katikati ya bahari, na kinataabika kwa mawimbi maana upepo ulivuma sana. Wakatazama na kuwaza "Yesu angekuwa hapa tungekuwa salama'. Ila Yesu hakuwa amewasahau marafiki Zake, baada ya saa sita usiku wanafunzi wakiwa wamefadhaika Yesu akawaendea akitembea juu ya bahari kama ardhi, wanafunzi wakashikwa hofu, wakifikiri ni kivuli au mtu, wakapiga yowe; wakijua nguvu ya uvutano haiwezi kumruhusu binadamu wa kawaida asizame au atembee kwenye maji.

Yesu akawaambia "Jipeni moyo ni mimi msiogope." Hata leo anatuambia maneno haya kila mmoja wetu. Yaseme kwa nguvu na yaamini. Petro akasema "Ikiwa ni wewe, niamuru nije kwako juu ya maji" huku nikitembea. Yesu akasema "Njoo", ndipo Petro akafanya lile ambalo binadamu hajawahi kufanya aliposhuka chomboni na kuanza kutembea juu ya maji.  Alitembea vizuri tu, mpaka alipoona hofu kwa kupungukiwa na imani. Pengine aliwatazama wenzake na kuwaringishia kwamba

yeye ndiyo 'mwenyewe' anatembea majini, badala ya kusifu uwezo wa Mungu. Basi akaona anaanza kuzama, na akapiga mayowe "BWANA niokoe." Hili limerekodiwa kama ombi fupi kupita yote kwenye Biblia.

Tukiomba hata ombi fupi, BWANA husikia, hasa ombi la kuokolewa kutoka katika uovu. Kuna maombi kadhaa ambayo Mungu hawezi kusema La! Hayo ni kama vile "BWANA niokoe toka dhambini au nisamehe. BWANA nionyeshe njia Yako ya kweli, au nionyeshe kama Upo. BWANA nifanye mimi kuwa chombo Chako. BWANA nifanye kuwa mkarimu. BWANA nionyeshe maumivu au masumbufu haya yana maana gani. BWANA naomba hekima. BWANA naomba ujasiri na uvumilivu. BWANA nionyeshe nimekuja hapa duniani kwa ajili gani. BWANA leta jambo jema katika machungu ninayopitia."

Basi Yesu alinyosha mkono Wake kwa Petro akamshika akisema "Ewe mwenye imani haba mbona uliona shaka?" nao walipopanda chombo upepo ulikoma, nao wanafunzi mwenye chombo walimsujudia wakisema "hakika Wewe u Mwana wa Mungu." Hapa Genesareti waliwakuta wale watu wawili ambao waliokuwa na pepo makaburini waliponywa na kuwa wamishonari. Watu walipowatambua Yesu na msafara Wake, walituma watu kwenda kote kando kando na kumsihi waguse hata pindo la vazi Lake tu, na wote waliogusa wakaponywa. Wamishonari walikuwa wamepeleka habari kote, Yesu na mitume wakaja kuvuna roho zenye thamani.

Siku ya pili yake watu walimtafuta Yesu. Hawakuona mashua ikiingia bali wanafunzi walikuwa peke yao, basi watu wakaenda Kapernaumu wakimtafuta Yesu, walipomwona wakasema "Rabi wewe umekuja lini hapa?" Yesu aligundua hawakumtafuta kupata wokovu, au kwa kuwa walitambua kwamba huyu ni nabii ila "kwa sababu walikula mikate na kushiba." Akawaambia chakula cha milele kidumucho cha kuhangaikia ni kile Mwana wa Adamu atawapa, yaani Maneno ya uzima ya Mungu. Wakauliza wafanyaje ili waweze kuzitenda kazi za Mungu? Naye akasema wamwamini Yesu aliyetumwa na Baba wa mbinguni. Wakasema baba zao walikula mana jangwani, na Musa aliwapa akiwaonyesha ishara.

Yesu akawaambia si Musa aliyetoa chakula bali Mwenyezi Mungu "Ndiye atoaye chakula cha Kweli kitokacho mbinguni." Watu wakataka chakula hiki ili wasiwe na njaa tena, Naye akawajibu "Mimi Ndimi chakula cha Kweli kitokacho mbinguni, Yeye ajaye Kwangu na kuamini hataona njaa wala kiu kamwe." Akasema "wote anipao Baba watakuja Kwangu wala yoyote ajaye kwangu sitamtupa kamwe." Yesu alikuja kufanya mapenzi ya Baba wa mbinguni, na hataki hata mmoja apotee kamwe, bali siku za mwisho afufuliwe kwa ufufo wa uzima, "amtazamaye Yesu na kumwamini Yeye, ana uzima wa milele, na Yesu atamfufua siku ya mwisho. Wayahudi wakachukia aliposema Yeye ni chakula toka mbinguni, wakisema "Huyu si mwana wa Yusufu, na mamaye twamjua?"

Yesu akawaambia hakuna awezaye kuja Kwake kama Mungu hakumvuta. Mungu Mwenyewe atatufundisha wanadamu. Yeyote amwaminiye yuna uzima wa milele. Yesu alijifunua kwa watu. Ilibidi mtu aweze kuongozwa na Roho ili aweze kumgundua, ila yule ambaye alikuwa hajamruhusu Roho wa Mungu kumwongoza

aliona giza. Yesu aliwaambia “Baba ampenda Mwana.” Akawaambia Baba wa mbinguni amempa hukumu YEYE. Asiyemweshimu Mwana hamheshimu Baba. Yeyote yule atakayesikia Neno la Mwana ana uzima wa milele na haingii hukumuni, ila amepita kutoka mautini na kuelekea uzimani. Kuna siku itakuja wafu waliolala mauti wataisikia sauti ya Mwana wa Adamu na kuinuka toka kwenye makaburi yao na kufufuka. Wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu.

Yesu akawaambia hawezi kufanya lolote bila mapenzi ya BABA Yake, na kuna mwingine aliyemshuhudia naye ndiye Yohana mbatizaji. Ila ushuhuda wa mwanadamu aliuzungumzia kwa maana walimjua Yohana na hili lingewapa kuamua kumfuata na kuokoka. Yohana alikuwa taa ya kung’aa, kwa muda na wakashangilia ila Yesu ushuhuda Wake ulipita wa Yohana, maana alikuwa Mwana wa Mungu.
Akawaambia, ”mwayachunguza Maandiko mkidhani kwamba yana uzima” ila Maandiko yote ya Musa na manabii yalimshuhudia Yeye. Ila aliwajua wao hawana upendo wa Mungu ndani yao maana alikuja kwa jina la BABA na hawakumpokea. Akawaambia Yeye hatawashitaki bali Musa ambaye wao wanamtumaini, kwa maana kama wanamwamini Musa hawawezi kuacha kumwamini Yeye “maana Musa aliandika habari zangu, lakini msipoyaamini Maandiko ya Musa, mtayaamini wapi Maneno Yangu?”

Maneno ya Mungu ni kama ngazi, au mnyororo, tusipoamini mafundisho ya nabii au fungu fulani, basi yote yanashindwa kufanya kazi. Na Amri Zake zote Kumi ni kitu kimoja, yaani ni kama kioo, kikivunjika kipande, ni kioo kizima kimevunjika!
*Omba, kisha; omba, nawe utapokea. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri na ongezeko la imani. Kwa kila ombi la dhati jibu litakuja. Linaweza lisije vile vile unavyotamani, au kwa wakati unaolitafuta jibu hilo; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao utakidhi mahitaji yako. Maombi unayotoa katika upweke, katika uchovu, katika majaribu, MUNGU hujibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini kila wakati kwa faida yako.
--------------------------------

Maswali: Kwa nini watu walitaka kumfanya Yesu awe mfalme? Kwa nini wanafunzi waliogopa walipoona mtu anatembea kwenye maji? Unafikiri ni kitu gani kilimzamisha Petro? Je waweza kukumbuka ombi fupi ulililoliomba? Yesu alijuaje watu hawa walikuwa hawana upendo wa Mungu ndani yao? Kwa nini watu wanapenda chakula kuliko Neno la Mungu? Je kusoma Neno la Mungu na kisha kula yaweza kuwa msaada kwa watu hawa?

**SIKU YA 233.**
**(Agosti 20)**

# Wanafunzi wanarudi nyuma na wengine watoroka.

**Yohana 6.**

Yesu aliwaambia kwamba mapenzi ya Mungu aliyemleta ni kwamba asimpoteze hata mmoja. Kila amtazamaye Mwana wa Mungu, ana uzima wa Milele. Wayahudi wengine wakamnungunikia kwa vile alisema Yeye ni "chakula kilichoshuka toka mbinguni yaani mkate wa mbinguni au Mana", wakisema "si mwana wa Yusufu na mamaye twamjua." Inakuwaje asema ameshuka toka mbinguni. Naye aliwaambia kila ajaye kwa Mungu si yeye ndiye amefanya jitihada ila Mungu Ndiye anavuta binadamu Kwake. Akasisitiza Yeye Ndiye Chakula cha Uzima toka mbinguni akimaanisha Neno la Mungu. Akawaambia watu kwamba mkate wa mana baba zao waliokula jangwani walikufa, ila Neno la Mungu wakila wataishi milele.

Wayahudi wakashindana "awezaje mtu huyu kutupa sisi mwili Wake ili tuule." Naye akarudia "Amini, amin nawaambieni, msipoula mwili wa Mwana wa Adamu na kunywa damu yangu hamna uzima wa milele, bali mkila mwili wangu na kunywa damu yangu mna uzima wa milele" na Yesu atawafufua siku ya mwisho wote, maana "Mwili Wake ni chakula cha Kweli na damu Yake ni kinywaji cha Kweli, Aulaye mwili Wake hukaa ndani ya Yesu na Yesu hukaa ndani Yake na kuwa hai." Kama Yeye alivyo hai ndani ya BABA wa Mbinguni. Aliyasema Maneno haya kama tamathali za semi au mafumbo akifundisha Kapernaumu kwenye sinagogi. Tunajua Mungu hataki tuule au tule watu, Yesu hakumaanisha kula nyama au damu za watu.

Hata siku ya leo tunajua kwamba kula watu ni dhambi, kwa wale wasiomjua Mungu, hawafanyi lile, kwa kutopenda na wakifanya wanapewa adhabu ya kifo, maana mtu yabidi auwawe ndiyo aliwe. Jamii fulani fulani kama ile ya Papua New Guinea ilijulikana kula watu kwa miaka mingi, hata katika karne yetu hii. Wamishonari wengi walipoenda kuhubiri waliuawa na kuliwa. Yesu aliposema Maneno haya, hakumaanisha kwamba wale nyama za binadamu. Bali wanafunzi waliposikia waliona Maneno haya ni magumu, "Ni nani awezaye kusikia?' wakajiuliza. Naye Yesu akijua Maneno haya yanawatatiza aliwaambia kama Maneno haya yanawakwaza basi itakuwaje watakapoona Mwana Adamu akipaa huko alipokuwako kwanza; Yesu akijua kati yao wengine hawaamini.

Kwa ajili hiyo miongoni mwa wanafunzi waliogopa kuwa watu wakarejea nyuma wasiandamane Naye, kisha Yesu aliwaambia wale 12 waliobaki "Je nanyi mwataka kuondoka?" Petro akajibu kwa ujasiri "Twende wapi BWANA Nawe una Maneno ya uzima wa milele, nasi tumesadiki na kujua kwamba wewe Ndiye Mtakatifu wa Mungu." Hapa ndipo alipoanza kuwafunullia kwamba mmoja wao atamsaliti. Inapasa

tuwe tayari kusikia Maneno ya uzima, kwani mara zingine utachanganyikiwa. Yesu aliposema wakachukulia maana yake halisi, wasijue ni msemo wa fumbo. Ilikuwa imefika wakati wa sikukuu ya makambi au vibanda, siku kuu hii ni mojawapo ya siku kuu kubwa tatu za Wayahudi zilizomwakilisha Yesu.

Wayahudi kwa upofu wao, walimtafuta Yesu wamwue. Ndugu Zake wakiwa wameshamwambia aende huko ili watu waweze kuona kazi Zake, na asifanye mambo kwa siri. Maana ndugu Zake hawakumwamini pia, mpaka alipokufa na kufufuka. Yesu aliwaambia wakati Wake bado kufika, na ndugu Zake walitangulia, Naye alikuja kwa siri baadaye. Wayahudi walianza kumtafuta kwenye siku kuu wasimwone. Wakati siku kuu ilipofika alikwea na kuingia hekaluni na akafundisha, wakashangaa "amepataje elimu Huyu ambaye hakusoma." Wengine wakashangaa mbona anafundisha wazi wazi, na watu wanamtafuta kumwua. Hawakufunuliwa kutokana na ugumu wa mioyo yao. Walidhani "Huyu si Kristo, maana Kristo akija hakuna atakayejua atokako." Walimtukana kwa kusema ni Msamaria mwenye pepo, na mengineyo. Walifungwa na macho ya kiburi na unafiki, bali watoto wadogo walifumbuliwa na kumwabudu Yesu. Walimtafuta kumkamata, lakini hakuna aliyeunyosha mkono wake kwa kuwa saa Yake ilikuwa haijaja bado. Ila wengine walimwamini, wakisema akija Kristo Je atafanya ishara nyingi zaidi ya hizi?

*Kufungua Moyo kwa Rafiki - Maombi ni kufungua moyo kwa MUNGU kama kwa rafiki. Sio kwamba tunamjulisha MUNGU jinsi tulivyo, lakini ili kutuwezesha kumpokea. Maombi hayamshushi MUNGU kwetu, bali hutupeleka Kwake. Wakati Yesu alipokuwa duniani, aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Aliwaelekeza kuwasilisha mahitaji yao ya kila siku mbele za MUNGU, na kupeleka mizigo yao yote Kwake. Na uhakikisho aliowapa ni kwamba maombi yao yatasikilizwa, ni uhakikisho pia kwetu.
--------------------------------

Maswali: Kwa nini ndugu Zake Yesu hawakumwamini? Kwa nini Yesu alikuwa na elimu japo hakusoma? Je! Ni lazima usome ndiyo uelimike? Elimu ni nini? Je! Unaweza usiende chuo kikuu na ukawa umeelimika kuliko yule aliyepitia chuo kikuu? Kwa nini wanafunzi wengine wa Yesu waliponyoka na kupotea? Petro alijibuje kwa ujasiri, alipoulizwa kama anataka kuondoka? Yesu alikuwa ana maana gani aliposema Yeye ni Mkate wa mbinguni na maji ya uzima?

**SIKU YA 234.**
**(Agosti 21)**

# Mwanamke aliyefumaniwa akizini.

**Yohana 8.**



Siku ya mwisho wa siku kuu Yesu alisimama na kupaza sauti akisema ”Mtu akiona kiu na aje Kwangu anywe.” Mtu amwaminiye atakuwa na maji hai, yaani kila anayemwamini atapokea Roho wa Mungu. Wengi wakamwamini, ila wengine walisema “Kristo hatoki Galilaya bali Bethlehemu” Hawakutaka hata kujiuliza kwamba ni kweli alizaliwa Bethlehemu bali alichukuliwa Nazareti Galilaya akiwa mdogo. Kila aliyemwomba Mungu amwonyeshe, alionyeshwa fumbo hilo. Baadhi wakitaka wamkamate walishindwa kunyosha mikono kumshika na watumishi waliotumwa na makuhani na mafarisayo walipoulizwa kwa nini hawakumkamata walijibu “Kamwe hajajibu mtu yeyote kama huyu alivyonena’. Na Hili ni Kweli, kwani kamwe hakuna aliyewahi kuishi na kutenda hapa duniani kama Yeye!

Hawa walikuwa wameshaonyeshwa kwamba Huyu ni Masihi. Ila mafarisayo wakawakashifu “Je ninyi nanyi mmedanganyika? Au Mnafikiri nyinyi ndiyo mna akili ya kujua mambo ya kiroho zaidi kuliko sisi?” Ndipo Nikodemu alipowaambia “Je sheria yenu inamhukumu mtu kabla ya kumsikiliza kwanza na kujua atendavyo.” Huyu alikuwa bado mwanafunzi wa Yesu kwa siri, akimpenda ila akiogopa watu

na akitafuta awapendeze watu kuliko Mungu. Wale makuhani na mafarisayo wakamjibu "Tafuta ukaone ya kuwa kutoka Galilaya hatatoka nabii yoyote!" Walikuwa wanasoma Maandiko yalijaa kwenye ubongo, ila mioyoni walijawa na chuki na uovu. Nao hawakujua kwamba Neno Mwenyewe Yu miongoni mwao, Naye alikuwa amevuvia watu kuliandika Neno, Naye alilijua lote! Na bado akazidi kujifunza kila siku. Watu masikini hawa hawakujua wanasimama na nani! Hata leo tunahitaji macho ya kiroho ili tumjue Mungu, na kwa kumjua, tuna uzima wa milele. Hata leo tunaposoma, Neno la Mungu si kwa ajili ya kujipatia maarifa tu, bali kubadilisha maisha yetu. Wangefanya hata utafiti mdogo tu kuhusu mahali Yesu alipozaliwa kama Maandiko ya Mika 5:2 yanavyosema, ingelikuwa rahisi kwao kumtambua. Hata hivyo Maandiko yanadhihirisha kuwa nabii Yona alitoka Galilaya, ila wao walisema hakuna nabii aliyetoka huko, haya yote yalionyesha ufinyu wa elimu yao. Wangemwomba Mwenyezi Mungu awaonyeshe wangeweza kujua Yesu ni nuru ya ulimwengu, na kila ajaye Kwake, hataona giza kamwe bali atakuwa nuru ya uzima. Mungu atusaidie kuondoa giza leo hii! Tusingoje kesho.

Yesu akaenda kulala mlima wa mizeituni, na asubuhi akaingia tena kwenye hekalu na watu wakamwendea awafundishe. Hapo ndipo waandishi wa sheria na mafarisayo wakamletea mwanamke aliyefumaniwa kwenye uzinzi, huku wakimburuza. Walimleta peke yake bila mwanaume, wakitaka kumjaribu Yesu wakasema katika torati "Musa alituamuru kuwapiga kwa mawe na kuwaua." Sheria ya Musa ilisema mtu apigwe mawe, ila walipaswa kuwaleta wote wawili, na kufungua mashitaka kwenye korti, na mashahidi, kisha ndiyo wapate adhabu hiyo. Walikuwa wamempa Yesu mtego, kwani adhabu ya kuuwawa siku zile walitawaliwa na Warumi, Warumi ndiyo walitoa adhabu ile, na hivyo sheria ya Musa isingeweza kufanya kazi. Na Yesu angesema wasifuate sheria ya Musa wangesema huyu si nabii wa kweli au mtu wa Mungu, bali msaliti wa imani ya Kiyahudi. Ila Yesu alijua moyo wa mwanadamu, wala hakuhitaji mtu amwambie anachofikiria, kwani akili zao zilianikwa wazi Kwake. Mwanamke huyu alikuwa akitetemeka, na nguo zake zimepasuka kwa kuburuzwa, akificha uso wake kwa aibu. Yesu alipowatazama wale washitaki wake, aliwaona watu wasiokuwa na huruma, na akajua walilokuwa wakiwaza. Kupungukiwa kwao kwa upendo kulimfanya awe na huzuni. Bila kujibu Yesu aliinama na kuanza kuandika mchangani. Hatujui aliandika Maneno gani, ila yaonekana maneno haya yaliwahukumu watu hawa wakajiondoa wenyewe. Ndipo Yesu akijua mioyo na mawazo yao yote, na hata nia yao ya kutaka kumshtaki kutokana na atakavyojibu aliendelea kuandika kwenye ardhi bila kuwajibu.

Watu hawa walijua kwamba hata wao si watakatifu na wana dhambi pia. Watu wengine wamefikiri pengine Yesu aliandika dhambi za kila mtu pale, kwa sababu walipoendelea kumhoji alisema "Yeye asiye na dhambi awe wa kwanza kumtupia jiwe", akainama tena na kuendelea kuandika. Watu hawa walishitakiwa na dhamiri zao, na wakatoka mmoja, mmoja na kuelekea kusokojulikana.

Yesu akainua kichwa na kumwona yule mwanamke pekee na akamwuliza "wako wapi wale washitaki wako? Je hakuna aliyekuhukumu kuwa mwenye hatia?" Yesu akamwambia yule mwanamke, kwamba hata Yeye hamhukumu. Akasema, "Enenda zako, wala usitende dhambi tena." Mwanamke huyu alikuwa Mariamu Magdalena,

yule aliyempaka marhamu miguuni. Dhambi ya kuzini inaeleta hofu, magonjwa, wasiwasi, kuzaa nje ya ndoa, kushitakiwa na dhamira, mawazo machafu, na hata kutengwa. Na siku ile dhambi ya kuzini ilikuwa inakaribia kumletea yule mwanamke kifo. Yesu hakumwambia aendelee na maisha maovu, la! Alimsamehe na kumwambia aache dhambi, ni Mungu tu awezaye kuweka yote sawa, rehema na haki!

Hata leo watu wengi wanauawa kwa kumchukua mke au mume wa mtu. Wengine wamepata maradhi ya akili kwa ngono haramu, au isiyoafikiana na Maandiko. Mariamu aliokolewa kutoka katika dhambi hii. Wengine wameingia dhambi kama hii kutokana na marafiki walio nao, au tamaa ya pesa. Sulemani anaonya wasichana wa rika moja wanaoingizana kwenye dhambi ya uasherati "Enyi binti Yerusalemu msichochee mapenzi kabla ya wakati." Si wavulana tu wanaoingiza wasichana kwenye dhambi hii bali marafiki wabaya wa aina yoyote, vijana na watoto mjilinde na marafiki waovu. Tunza usafi wa moyo, maneno, na matendo. Mvulana au msichana akikushawishi kufanya dhambi hii, mwambie mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu, na ujitunze kwa usafi mpaka siku ya arusi yako. Usisite kuwaambia wazazi wako, walezi au mtu mzima ambaye anaonekana kumpenda Mungu, pale unapoona kuna hatari ya aina fulani.

Yesu alifikia watu wa kila aina; wanaume, wanawake, matajiri, masikini, wafupi, warefu, wageni, na wenyeji. Nasi leo tunapaswa kufikia watu wa aina zote, tusiogope! Yesu hakukubaliana na dhambi. Alichukia dhambi, ila alimpenda mwenye dhambi. Yesu alijali sheria za Musa, hata walipomleta Mariamu, kwani hakukutokea mashahidi wawili walioafikiana kwamba mwanamke huyu aadhibiwe, wote walipotea. Yesu alikuja kufa kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe kutoka katika dhambi. Dhambi ni jambo zito, ila Mungu anatuhurumia kwa ajili ya udhaifu wetu, mpango Wake ni kutuokoa na udhaifu unaotuzinga kwa wepesi kila mmoja wetu.
Mariamu hakuambiwa arudie maisha yale ya dhambi, bali aliambiwa aende na kubadilika kwa neema ya Mungu. Mungu wetu ana hekima na rehema za peke yake. Baada ya kusoma habari hii nadhani wote tutakuwa waangalifu kuwa na rehema zaidi kwa walio katika makucha ya Shetani. Maana wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Tunapoona udhaifu wetu tunamwomba Mungu atupe ushindi ili tuachane na dhambi. Pia wengine wenye udhaifu wa dhambi tunawaombea na kuwasaidia. Pengine ni mzazi mwenye hasira, au kaka mwenye tabia ya udokozi, wote hawa wanahitaji rehema zetu na kuwasaidia waache tabia mbovu.

Kosa baya lililofanywa na watu waliomleta yule mwanamke aliyefumaniwa ni kwamba, baada ya Yesu kuwaonyesha makosa yao ndani ya mioyo yao, badala ya kuungama na kutubu, wao wakatimua mbio toka kwa Yesu. Kumbe kuna hatari ya watu wengi kukaribia kabisa wakovu na ghafla wakaondoka bila kuokolewa! Leo ukiona rafiki yako wa karibu anatenda dhambi omba, na kisha kwa upendo mweleze au mwelekeze, utakuwa umeokoa roho. Ila usimsengenye au kugombana naye, akisikia atakuwa amebarikiwa na atatubu, na kubadilisha mwenendo wake. Sisi ni walinzi wa ndugu zetu, ila uliza hekima toka kwa Mungu kwanza jinsi ya kushugulikia jambo hili.

* "Njooni Kwangu," ndio mwaliko Wake Mungu. Ikiwa una wasiwasi na majaribu yoyote, wasilisha shauri lako mbele za Bwana. Kuna watu wachache wanaothamini au kuboresha upendeleo wa thamani wa maombi tuliopewa na Mungu. Tunapaswa kwenda kwa Yesu na kumwambia mahitaji yetu yote. Tunaweza kumpelekea wasiwasi, masumbufu au fadhaa zetu ndogo na mashaka pamoja na shida zetu kubwa. Chochote kinachojitokeza kutusumbua au kutufadhaisha, tunapaswa kukipeleka kwa Bwana katika maombi. Tutakapohisi kuwa tunahitaji uwepo wa Kristo katika kila hatua, Shetani atakuwa na nafasi ndogo ya kupenyeza majaribu yake. Ni juhudi yake ya makusudi kutuweka mbali na rafiki Yetu bora na mwenye huruma. Hatupaswi kumfanya mtu yeyote kuwa msiri wetu ila Yesu. Tunaweza kuzungumza Naye kwa usalama, yale yote yaliyomo ndani ya mioyo yetu.


-------------------------

Maswali: Kwa nini ni vyema kumruhusu Roho wa Mungu atusaidie tunaposoma historia? Je Yesu alisema aliafikiana na dhambi ya Mariamu? Kwa nini watu walitoweka na kupotea Yesu alipoanza kuandika chini? Watu wamesema Mungu anaandika dhambi kwenye mchanga ila sheria Zake aliziandika kwenye mawe, hii ina maana gani kwetu? Je kuna watu wenye dhambi darasani au karibu yako unaoweza kuwafikia?

**SIKU YA 235.**
**(Agosti 22)**

# Kipofu aponywa.

**Yohana 9.**



Yesu aliendelea kufundisha ndani ya chumba cha hazina cha hekalu kwenye siku ya vibanda kwamba Yeye ndiyo nuru ya ulimwengu, na ushuhuda wake ni wa kweli. Akawambia anajua anakotoka na anakokwenda ila wao hawajui, alipotoka au anakokwenda. Naye akasema akiondoka watamtafuta. Maana aendako hawawezi kumpata, na hiyo ikawafanya wajiulize kwamba anaenda wapi. Akawaambia Yeye ni wa mbinguni na wao ni wa chini, watakufa na dhambi zao wasipomkubali na kumwinua Yeye "Mwana wa Adamu." Hata wale marafiki Zake wa karibu hawakujua anaenda wapi, wakasema pengine aenda Uyunani, au Uitaliano.

Akawaambia watakaomwamini watakuwa wanafunzi Wake, na watakuwa wametoka kwenye utumwa, maana kutenda dhambi ni kuwa utumwani. Hapo walisema wao ni wana wa Ibrahimu hawawezi kuwa watumwa. Wakadai baba yao ni Ibrahimu. Hapo Yesu aliwaambia, "Kama mngekuwa watoto wa Ibrahimu msingetaka kuniua Mimi, maana Ibrahimu hakufanya hivyo." Ibrahimu alimpenda Mungu, na kushika maagizo Yake. Kama wao wangekuwa na mawazo ya mbingu wangempenda Mungu na Mwana Wake aliyemtuma, na kuyaelewa anayowaambia.

Akawaambia wazi kabisa kwamba mtu anayekataa mafundisho Yake na ya Baba Yake ni wa Ibilisi na si wa Mungu. Maana walihusika na kuua watu na kusema uongo kama Ibilisi, na wala hawakutenda kama Maandiko yalivyoagiza. Na hapo alipowaambia kwamba "Ibrahimu alishangilia kuiona siku Yake na akafurahi." Nafikiri hapa ni pale Yesu alipomwona Ibrahimu akiruka ruka kwa furaha, akiwa mbinguni alipojaribiwa kutoa kafara ya mwanawe bali Mungu akamwonyesha mengine mengi mazuri. Ibrahimu alionyeshwa wakati huo, Yesu atakavyojitoa na hakuwa na haja ya kumchinja tena Isaka. Si kwa sababu ya yule kondoo dume aliyekwama pembe zake kwenye kichaka, bali kwa ajili ya Kafara ile kubwa na halisi yaani Yesu, atakavyoitoa ili sote tusiangamie.

Walishangaa kwamba hajapata miaka 50 na ameshamwona Ibrahimu! Hapo ndipo Wayahudi wakasema "Wewe u Msamaria na una pepo." Naye akawaambia "Amin amin, yeye Ibrahimu asijakuwako, Mimi Niko." Hapo ndipo walipookota mawe wamtupie, maana walijua vyema 'MIMI NIKO' aliyoambiwa Musa na Mungu, ndiyo Jina alilotumia Mungu. Yesu hapa alijidhihirisha wazi kwamba Yeye ni Mungu Yule aliyewaongoza wana wa Israeli jangwani. Yesu akatoka hekaluni kwa uwezo wa Mungu wasimwone.

Katika juma hili, wakati Yerusalemu, siku kuu ya vibanda ikiendelea, Yesu aliwaambia Yeye ni Nuru ya ulimwengu, kwamba mtu atakayemfuata hataona giza kamwe au kujikwaa, maana atamwongoza kwenye uzima wa milele; basi tukae katika ile nuru. Alipokuwa akipita alimwona mtu aliyekuwa kipofu toka kuzaliwa. Wanafunzi walitaka kujua kwa nini alikuwa kipofu. Je ni kwa ajili ya dhambi zake au za wazazi wake. Hata leo nawe utakuwa unataka kujua jibu la swali hilo!

Swali kama hilo pia aliulizwa Yesu wakati machafuko yalipotokea hekaluni na Pilato alituma jeshi kwenda kule na lilipofika liliua kila mmoja, wakiwemo wahujaji wa Galilaya. Yesu akawauliza mnafikiri wao ndiyo walikuwa wabaya kuliko watu wengine na ndiyo maana Mungu akaruhusu haya kutokea? Akawaambia, mnafanya makosa kufikiri vile. Maana walifikiri matukio mabaya au ajali huwatokea watu kama adhabu ya uovu wao. Akawatahadharisha kwamba wasipoacha kuhukumu tabia za watu kwa yale mabaya yanayowatokea, basi kuingia mbinguni kwao mbinguni kutakuwa kazi. Akatoa mfano mwingine wa mnara Siloamu uliowaangukia watu 18 wakafa wote wakijenga, si kwa kuwa walikuwa waovu zaidi.

Wengi wamejiuliza leo, kwa nini mtu anazaliwa na kilema au kwa nini watu hutokewa na jambo baya? Si mara zote kutokea kwa jambo baya hutokana na adhabu ya Mungu kwani tunaishi katika dunia ya dhambi, na katika pambano kuu kuna sheria za vita (rules of engagement) ambazo hatuzielewi vizuri, soma somo la namba 159 kuhusu kisa cha Ayubu, na kisha kitabu kinachoitwa Pambano Kuu kati ya Mungu na Shetani, kipo mtandaoni. Ila mara zingine dhambi zinafanya mabaya kutokea, mfano mama anayekunywa pombe wakati wa ujauzito, anamdhuru mtoto wake aliye tumboni, na mtoto huyo aweza kupata ulema, Au mtu ambaye ni mlafi, anaweza kupata uzito mkubwa na kuugua kisukari au presha, na kisha mwili ukapooza, na kupata ulema. Basi Yesu alijibu akisema mtu yule aliyefikwa na mabaya hakutenda dhambi, wala wazazi wake, bali ili "kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake", yaani utukufu, ukuu na uponyaji Wake. Yesu akaendelea kusema, "imenipasa kufanya kazi zake Yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana, usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi." Alisema hayo huku akiinama na kuchukua udongo alioufanya tope kwa mate, na kumpaka kipofu macho yake, na kumwambia akanawe kwenye birika la Siloamu. Mtu huyu alienda, na kisha kurudi akiwa anaona; mtu ambaye jirani zake hapo zamani walimtambua kama 'omba omba.'

Hawa walishangaa kama ndiye yule kweli. Macho ni kitu cha thamani, na mara nyingi tunajaribu kuyalinda ili michanga au kitu kisichotakiwa kisiyadhuru. Mtu huyu alifurahi ameweza kuona. Wengine wakasema huyu siye yule waliyemfahamu, ni mwingine amefanana naye tu. Walipomwuliza yeye alisema "mimi ndiye."

Wakamhoji nini kilitokea, naye akasema “Mtu aitwaye Yesu, alimponya” kisha akaelezea jinsi alivyoweka tope kwenye macho na kumwagiza kunawa, naye akaweza kuona. Wakamwuliza Yesu Yupo wapi, ndipo walimchukua yule aliyekuwa kipofu kwa mafarisayo wamshtaki Yesu kwa kuponya siku ya Sabato. Wakamchukua pembeni tena. Walipofika huko wakaanza kumwuliza aeleze tena ilitokeaje. Akaeleza, lakini baadhi ya mafarisayo waliendelea kudai kuwa Yesu hatoki kwa Mungu kwa sababu ameponya siku ya Sabato. Naye yule mtu akasema kama hatoki kwa Mungu na ni mwenye dhambi, “awezaje kufanya ishara kama hizo?”

Mtu huyu alikuwa kipofu ila ubongo wake ulikuwa unafanya kazi vyema. Kukawa na kufarakana kati yao wenyewe na wale wanaomhoji. Kisha wakamwuliza yule kipofu tena aeleze uponyaji ulivyotokea na kama yule mtu ni nabii. Kipofu wa watu akifurahia kuona jua, rangi, watu na maumbo kwa mara ya kwanza alishangaa wale watu walivyokuwa wanashughulikia mambo madogo akafikiri ni wapuuzi, ila kwa sababu walikuwa viongozi akajikaza awaheshimu. Akawaambia kwamba Yesu “ni nabii”, ila hawakumsadiki, na kisha waliita wazazi wake, na kuwauliza kama alikuwa mwana wao, na alizaliwa kipofu au ni porojo tu. Wazazi wakajibu ‘ndiyo’, alizaliwa kipofu. Waliwauliza, nini kimetokea akaona. Basi wale wazazi wakiogopa kutengwa kwenye sinagogi au jumuiya endapo watamkiri Yesu kuwa ni Kristo, wakasema “ni mwana wetu, alizaliwa kipofu, hatujui ni nani alimfumbua macho, mwulizeni yeye mwenyewe, yeye ni mtu mzima, atajisemea mwenyewe.”

Kipofu akaendelea kumshukuru Mungu, kwani sasa aliweza kuona maua, anga, wazazi wake, ndugu, marafiki, maji, na vitu vyote ambayo toka kuzaliwa hakuwahi kuviona. Alikuwa kwenye darasa la ugunduzi wa vitu vingi, akiuliza hiki ni nini, kile ni nini? Alikuwa amepata nuru toka kwa Yesu, pengine ndiyo uso wa kwanza kuuona katika maisha yake! Hili latuvuta tujifunze kufurahi na wenzetu wanapokuwa na furaha na si kushughulikia mambo ambayo hayana msingi kwa mabishano; kama kusema anadanganya alikuwa anaona kabla.

*Wakati Yesu alipokuwa duniani, aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Aliwaelekeza kuwasilisha mahitaji yao ya kila siku mbele za MUNGU, na kupeleka mizigo yao yote Kwake. Na uhakikisho aliowapa ni kwamba maombi yao yatasikilizwa, ni uhakikisho pia kwetu.
-----------------------------

Maswali: Kwa nini watu wanapenda kujisifia ni watoto wa Ibrahimu ila wanatenda kinyume cha Ibrahimu? Kipofu aliambiwa aende kuosha macho yake wapi? Kipofu aliweza kuona mambo gani kwa mara ya kwanza? Yesu alijibuje swali la mtu kuzaliwa kilema?

**SIKU YA 236.**
**(Agosti 23)**

# Kipofu aliyefumbuliwa macho atengwa ushirika.

**Yohana 9.**

Wakamwita yule kipofu, baada ya kuhoji wazazi na kumwambia ampe Mungu utukufu kwa kuona, na si kumpa utukufu Yesu kwa vile ni mwenye dhambi. Yule mtu alijibu "Kwamba Yesu ana dhambi sijui ila neno moja najua, nalikuwa kipofu na sasa naona." Wakamwuliza alikutendea nini? Hapo yule mtu alichoka, kwani alikuwa amefanyiwa muujiza wa ajabu, ila walitaka kumsumbua kwa chuki yao kwa Yesu na kutoamini. Hawa watu walikuwa na upofu zaidi ya huyu kipofu wasijue. Hapo ndipo alipowaambia "Nimekwisha kuwaambia, bali hamkusikia, Je mnataka kuwa wanafunzi wake?" kufikia hapo wakaanza kumshutumu kwa hasira wakisema, "sisi ni wanafunzi wa Musa, hatujui Yesu alipotoka."

Watu hawa walikuwa vipofu zaidi ya yule mtu, wasijue mbele yao alikuwa anasimama Mkuu zaidi ya Musa. Watu hawa walikiri kwa akili zao kuwapo kwa majina, miji, na matukio ya historia yaliyokuwa kwenye Biblia, ila mioyo yao haikuguswa. Yule mtu akawauliza, inakuwaje hawamjui Yesu atokapo, Naye Ndiye aliyemfumbua macho? Akaendelea kusema anajua Mungu hasikii maombi ya wasio wacha Mungu na wasioyafanya mapenzi yake, imekuwaje basi sasa yeye anaona? Mbona haijawahi kusikiwa kuwa mtu amefumbuliwa macho, ambaye alizaliwa kipofu, na mtu ambaye anadhaniwa hakutoka kwa Mungu? Wakamwambia "ulizaliwa na dhambi unatufundisha nini" wakamtoa nje ya ushirika.

Yesu alisikia walichofanya na alipomwona alimwuliza "Wamwamini Mwana wa Mungu?" Naye akajibu "Ni nani nipate kumwamini." Yesu akamwambia, "umemwona, naye ndiye anayesema nawe." Ndipo yule mtu akamsujudia. Yesu akasema amekuja duniani kufanya wasioona waone. Mafarisayo waliosikia vile wakasema kwa kujishuku "Je sisi nasi tu vipofu?" Akawaambia kama wangekuwa vipofu wasingekuwa na dhambi, ila kwa kuwa wanasema wanaona na hali wao ni vipofu, hivyo wana dhambi kubwa. Tukimsimamia Yesu bila aibu wala woga kama alivyofanya yule kipofu, Yesu anaahidi kutusimamia. Yesu alipozungumza na watu alijua mioyo yao, na kwa mioyo yenye hila walijihukumu.

Akawambia wale walimu wa ile Kweli yaani Maandiko wanaingia kupitia mlango wa zizi ila wezi wanaiba washiriki kwa kuvunja nyumba au kupitia pengine. Yesu akasema Yeye Ndiye mchungaji wa Kweli wa kondoo, Naye huita kondoo kwa majina yao, naye huwatangulia na kondoo humfuata, kwa maana waijua sauti Yake. Akitokea mgeni, kondoo watamkimbia, maana sauti Yake hawaijui. Wale wanaochunga wanajua jinsi mchungaji anavyopenda mifugo yake na kuishughulikia mno. Hata leo makanisa mengine yanafuta watu ushirika si kwa vile wamefanya

dhambi au kuvunja amri, ila kwa sababu wakuu wa hilo kanisa wana njia za giza au uovu wa aina fulani. Hawa wanamchukia mtu yule na kutaka wamtoe machoni pao. Ni muhimu tusifuate mapokeo ya mtu, au ya kanisa, bali tumtafute Mungu na Neno Lake. Kila mtu ni muhimu awe kwenye ushirika unaoufuata Neno la Mungu, yaani Biblia, na kujihadhari na mapokeo au mafundisho ya watu au kanisa. Kila kanisa lina mapokeo fulani ambayo si mazuri kama ambavyo Wayahudi walivyofanya. Inabidi kila kanisa lijichunguze na kuachana na mazoea au mapokeo yanayopingana na Neno la Mungu. Cha kutia moyo ni kuwa, Yesu alipokea ibada ya mtu huyu kipofu wakati alipomsujudu na kumwabudu, ingawaje alikuwa ametengwa ushirika. Sishauri mtu yoyote ajitenge na ushirika wa kanisa maana Waebrania 10:25 inasema ni muhimu kuhudhuria ibada. Bali endapo ikitokea umefukuzwa kanisa fulani kwa ajili ya ubaya wa watu hao na si dhambi yako, basi jipe moyo ukijua hayo yalikuwepo toka zamani. Ila kama umesimamishwa ushirika kwa dhambi zako, tubu na ufuate njia za Maandiko na kurudi kwenye ushirika tena.

Leo tunaweza kutofautisha mtu asiye wa Mungu, awe kiongozi wa kiroho au mshiriki wa kawaida, kutokana na mafundisho au tabia yake. Yesu aliposema haya wengi hawakuelewa. Ndipo aliposema Yeye ndiye mlango, na mchungaji mwema. Si mchungaji wa mshahara akitamani pesa za watu, bali anayejali uzima na maisha ya roho zao. Mtu wa mshahara akiona mbwa mwitu amekuja kuchukua kondoo hukimbia ajisalimishe mwenyewe, kisha kondoo huraruliwa. Yesu Ndiye "mchungaji mwema, na kondoo walio Wake wanaijua sauti Yake." Naye akasema atatoa uhai Wake kwa ajili ya kondoo, au kwa ajili yetu wanadamu ili tupone kutoka katika dhambi.

Yesu akasema ana kondoo wengine pia ambao si wa zizi hili "yanipasa kuwaleta na sauti yangu wataisikia, kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja." Akimaanisha kwamba japo wengi hawamjui Mungu na Yesu, kama tunavyomjua, kwa vile hawakupata nafasi ya kuambiwa; basi kuna siku hawa wa 'kundi jingine' watapata habari wakiambiwa na watu, au kusikia redioni au kwenye vitabu nao watajiunga na kundi lile la Mungu. Watu hawa ambao hawajapata habari, wanafanya mema na kutimiza maagizo ya Mungu kutokana na Maandiko waliyofanikiwa kuyapata.

Wako wengi siku hizi wanaoabudu miungu mingine bila kujua, kama vile dini ya Hindu, na Budha. Hawa ni wengi sana, wanaweza kufika bilioni mbili. Wapo wengine pia wanaomwamini Mungu wa mbinguni bali kuyaelewa Maneno Yake vyema na jinsi tabia yake ilivyo. Hawa pia Mungu atawafikia ili wote tuwe kundi moja. Mungu ni mmoja, na mafundisho Yake hayatofautiani, ila sote ni lazima tuwe wanyenyekevu na kuwa tayari kujifunza kwa kuwa kuna Mungu mmoja tu dunia nzima na paradiso pia ni moja. Sote ni watoto wa mmoja, hivyo daima tuwe wanyenyekevu kujifunza kutoka Kwake, na si kusikiliza mapokeo yetu, dini yetu, au kung'ang'ania kile ndugu zetu walichotuambia. Tujikite katika "Imeandikwa" yaani katika Neno la Mungu. Daima tupende kuwavuta wengine wamjue Mungu, na kuwaombea twende nao mbinguni wakati Yesu arudipo.
Watu wengine walisikiliza wakaingiwa na Shetani na kusema "ana pepo ama ana wazimu, msimsikilize." Wengine wakasema "Maneno hayo siyo ya mtu mwenye

pepo. Je pepo aweza kuwafumbua macho vipofu? Yesu akawaambia kwamba Yeye na Baba wana umoja. Wayahudi wakaokota mawe ili wampige, akawaambia “kwa kazi zipi mnataka kunipiga mawe?’ Nao wakajibu kwamba tunakupiga kwa sababu “Wewe uliye mwanadamu wajifanya Mwenyewe u Mungu” Walidai kuwa anakufuru kwa kujiita Mungu. Waliposoma unabii wa Masihi hawakuelewa kutokana na mioyo yao kuwa migumu. Walishangaa kuona kuwa hapakuwapo na binadamu aliyezungumza na kufanya kama Yeye. Hata leo Yesu bado ndiyo mtu mashuhuri kupita wote, kwani miaka yote Kabla ya Kristo na baada ya Kristo, historia yote imejikita katika maisha Yake. Yeye ni Mwana wa Mungu, hatupaswi kamwe kumlinganisha na mwanadamu. Wengi leo wanamjadili na kujiuliza kama kweli ni Mwana wa Mungu, Mkombozi au BWANA? Jibu Yeye ni Yote hayo.

Tuwe makini tusiwe na uhodari wa kuropoka maneno na kutukana watu wa Mungu, bali tuwe wapole kujifunza Neno Lake kwa unyenyekevu. Wayahudi walijipinga, na huku wakajua kwamba wana mapungufu fulani katika mitazamo yao hawakutaka kubadilisha mapokeo yao mazito yaliyokuwa hasi. Yesu aliwaambia kama Yeye anatoa pepo kwa nguvu za Shetani, itakuwa ni maajabu, maana mapepo au majini ni Shetani na wafuasi wake, sasa itakuwaje ayakemee na kuyafukuza yaende, ikiwa anayafanyia kazi au yuko upande wao? Busara ingekuwa ayakaribishe yakae zaidi kwa watu hao, ili Shetani na ufalme wake ushamiri na kunawiri.
Akaenda ng’ambo huko na watu walimwendea na kusema Naye. Yohana mbatizaji naye aliendelea na kazi, naye hakufanya ishara au miujiza ila yote aliyosema kuhusu Yesu yalikuwa Kweli”, wengi wakamwamini kule. Hata leo yawezekana tusifanye miujiza ila yote ambayo tutasema kuhusu Mungu yawe ya kweli, na matendo yetu yawe na mvuto mwema, tutavuta wengi Kwake.


*Maombi yetu siyo mzigo kwa Mungu na Yeye hachoshwi nayo kamwe— Hakuna wakati au mahali ambapo hapafai kutoa sala kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika roho ya maombi ya bidii na dhati. Katika umati wa watu mitaani, katikati ya biashara au shuguli, tunaweza kutuma maombi yetu kwa MUNGU na kuomba mwongozo Kwake, kama vile Nehemia alipofanya ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kufungua mlango wa moyo kila wakati na kutoa mwaliko wetu kwenda juu ili kumwalika Yesu aje kukaa kama mgeni wa mbinguni katika mioyo yetu.
-------------------------

Maswali: Kwa nini yule kipofu hakutaka kuwasikiliza wale waovu? Je Yesu angefanya kazi leo, na kutembea duniani kama siku zile angekumbana na changamoto gani? Mchungaji wa mshahara ni nani? Kondoo wengine ambao si wa zizi hili ni wapi? Kwa nini ni kufuru na uongo kusema kwamba Yesu ana pepo au wazimu? Mafarisayo walikuwa na upofu gani?

**SIKU YA 237.**
**(Agosti 24)**

# Mwenye pepo Gerasi.

**Marko 5, Mathayo 8. Luka 8.**




Wakafika ng'ambo ya bahari baada ya tufani kukemewa, katika nchi ya Wagerasi. Waliposhuka chomboni, walikutana na watu wawili wametoka makaburini wenye pepo mchafu. Hawa walikaa kaburini na hakuna aliyeweza kuwafunga, hata minyororo na pingu nyingi walizikata. Hakuna aliyekuwa na nguvu kuwashinda. Ukiwatazama usoni walitisha, hata unaweza kujiuliza hawa ni watu kweli au ni nini? Walikuwa wakali, hakuna mtu aliweza kupita njia hiyo. Watu wengine waishio mijini wameona watu wenye magonjwa ya akili, wakawaita 'wenda wazimu' walipoona matendo yao.

Hata nami nimekimbizwa mara kadhaa na watu kama hawa, na kisha kupigwa nikienda shule darasa la tatu kule mjini Mbeya. Kila mahali kuna wagonjwa kama hawa ambao wanasikitisha kwa kuteswa kimwili na kiroho, na jamaa zao wanashindwa kuwasaidia maana wanakuwa na nguvu, na hawakubaliani nao. Nchi za magharibi huchukua polisi na kuwapeleka watu hawa kwenye mahospitali kwa nguvu, kwa kuwafunga au kuwapa dawa fulani. Zamani zile hiki hakikuwepo.

Basi watu hawa walikaa usiku na mchana kaburini na milimani wakipiga makelele na kujikata kata kwa mawe. Shetani anatesa watu hata siku hizi kwa mapepo. Mapepo ni wafuasi wa Shetani, yaani wale malaika waliaoanguka wa Ufunuo 12. Watu hawa wawili walipomwona Yesu, yale mashetani yanayokuwa yanawamiliki, yalitumia midomo yao na kupiga kelele kwa sauti kuu yakisema "tuna nini Nawe Mwana wa Mungu hata umekuja ututese", kwa sababu Yesu aliyaamrisha "Ewe pepo mchafu watoke watu hawa." Yesu akauliza mapepo, majina yao ni kina nani? Nao wakasema ni legioni, ikimaanisha walikuwa kundi kubwa la malaika wa Shetani wakiishi ndani ya mtu huyu. Yawezekana walikuwa 2,000 au zaidi.

Pepo wakamsihi Yesu, wakitoka ndani ya wale watu, waende kwa nguruwe, maana walijua hapa kuna Mwenye Mamlaka na Milki zote, yabidi wasalimu amri na kuomba ruhusa. Yesu akawapa ruhusa, nao pepo wachafu wakaingia katika wale nguruwe, na wakafanya wale nguruwe waharibikiwe na bongo zao, wakaanza kutelemka

kilima kwa kasi, wakaingia baharini, na wale nguruwe wapatao elfu mbili hivi wakafa baharini. Wachungaji waliokuwa wakiwachunga wakakimbia wakieneza habari hii mjini na mashambani. Watu walishikwa na hofu ya mambo ya ajabu yaliyotendeka. Wenyeji hawa waliagizwa kwa wazi kwamba wasifuge au kula nguruwe, lakini wao walikiuka amri ile. Lazima siku iliyofuata, maji yote yalilijaa nguruwe walioelea, katika nchi ambayo watu walikuwa hawatumii nguruwe, basi kilikuwa kitu cha kusimulia.



Watu wakamwendea Yesu na kuona wale wenye mapepo wametulia, wamevaa nguo, na wana akili zao. Hawa ndio waliokuwa na lile jeshi la mapepo. Wale watu wakaogopa. Watu walisimuliana, na kushukuru jinsi wale watu walivyopata uponyaji; ila wale wenye nguruwe waliona mradi wao umeharibiwa, wala hawakuwafikiria wenzao waliokuwa wameteswa na kufunguliwa. Pochi zao au nguruwe vilithaminiwa zaidi; japo walikuwa wanyama najisi waliokatazwa wasiliwe. Watu walikaidi agizo hilo wakitaka kujipatia faida nono. Basi mji wote ukaja kumlaki Yesu na kumsihi aondoke mipakani mwao, asije 'kuwatia hasara zaidi.' Hawakufikiria wokovu wao au hata kufikiria kumwalika aje kuwasaidia kuponya wagonjwa wao, bali wao walifikiria fedha zaidi.

Yesu akipanda chomboni, wale wenye pepo walimsihi wafuatanaye ili wawe wanafunzi Wake, ila Yesu aliwaambia waende kwa watu wa nyumbani mwao, na kuwaambia mambo makuu Mungu aliyowatendea na kuwarehemu. Ufunuo 12:11 yasema watu "wakamshinda Shetani kwa damu ya Mwanakondoo na ushuhuda wa neno lao." Hawa wenye pepo walioponywa walikuwa mitume wa kwanza ambao Yesu aliwatuma waende! Walifanya kazi njema; Wakaenda kwao Dekapolisi (miji kumi) kuhubiri mambo makuu Yesu aliyowatendea na watu wote waliowajua wakastaajabu. Yesu aliporudi kwao tena baaada ya miezi sita, alikuta waliompokea kutokana na ushuhuda wa hawa wenye pepo waliopona. Hawa watu waliomwambia Yesu atoke, asikae karibu yao, Yesu aliwakuta wanamngoja Gerasi/Gadara tayari kumwamini na kumfuata.

Pepo wachafu wapo wengi hata leo hii. Pepo ni maajenti au malaika wa Shetani, kati ya wale waliotupwa mbinguni na Shetani wanaotajwa kwenye Ufunuo 12. Injili inasema kuhusu mapepo yaliyotolewa na Yesu. Shetani na malaika zake wanajua fika Yeye ni nani, wanajua waliumbwa Naye kama malaika wa nuru, mpaka walipochagua kuasi na kuumiza wanadamu. mashetani yalikuwa na bidii Yesu alipokuwa duniani, wakitaka waharibu kazi ya wokovu toka kuzaliwa Kwake Yesu mpaka alipokufa. Mapepo kama Shetani ni adui za Mungu na adui zetu.

Mapepo ni waovu na wanataka kuangamiza binadamu. Tuvae silaha za Mungu. Kusema kwamba Shetani au mapepo hayapo ni hatari maana ni vyema kujua kuwa adui yako yupo, ila usibakie hapo ni lazima upige hatua kwa kumfuata na kumtii Mwenyezi Mungu.

Ni muhimu ujue kwamba Mungu ana uwezo wote, nguvu zote, maarifa yote, na ana uwezo wa kuwa mahali popote na wakati wowote. Shetani ana maarifa na uwezo ule tu ambao Mungu amemruhusu awe nao. Mungu anatamani tupate wokovu, kuliko kitu kingine chochote, ndiyo maana akamtoa Kristo Yesu. Yeye anatupa nguvu kila siku ya kumpinga Shetani tukichagua kuwa upande Wake. Kama mapepo au Shetani ana nguvu, YESU ana nguvu zaidi. Kila mahali Yesu alipokutana na mtu mwenye pepo, alimtoa pepo na kumwamurisha apotee. Hivyo basi, yeyote ambaye amemchagua Yesu kuwa Mwokozi na mtawala wa maisha yake, Yesu anao bado uwezo wa kumkinga mtu huyo na pepo lolote lile. Kama Yesu ni Mwokozi wako, amini kwamba huna haja ya kuogopa mapepo wachafu, maana kwa Jina lile tukufu la Yesu, mapepo wanakimbia mbali.

Tunajifunza kwamba mambo mema yalitokea pale ambapo watu walikuwa tayari kuwajulisha wengine matendo makuu ya Mungu. Je nawe Mungu amekutendea mambo makubwa? Usisahau kuwasimulia watu mambo hayo. Usipunguze nguvu za matendo makuu Mungu aliyokutendea. Watu walioponywa magonjwa husema "Nilikuwa na tabibu mpasuaji mzuri", kumbe ni BWANA amewasaidia. Wengine baada ya kushindwa mitihani mara nyingi, na wakamwomba Mungu wakafanya vizuri, husema "Nina akili nyingi au ni bahati yangu tu." Wengine wakiona wanapata kazi nzuri, husema "nina ustadi mwingi na binamu yangu amenisaidia kupata hii kazi."

Je Mungu amekupa akili njema? Je amekusaidia kuacha hasira mbaya? Je amekusaidia kuachana na tabia mbaya? Waambie watu mema hayo. Ni nani ajuaye ushuhuda wako wa ajabu utaleta mamia kwa Mwenyezi Mungu?

*Wacha roho ivutwe na kwenda juu, ili MUNGU atupe pumzi ya anga la mbinguni. Tunaweza kukaa karibu na MUNGU ili kwamba katika kila jaribu lisilotarajiwa mawazo yetu yatamgeukia Yeye kama asili ya ua ligeukiapo jua (automatiki!).

----------------------------

Maswali: Kwa nini wenye pepo walikaa makaburini? Wenye pepo walisema nini walipomwona Yesu? Je tunajuaje kwamba Shetani yupo? Mapepo maana yake ni nini? Je Kwa nini wenye pepo walitaka kumfuata Yesu? Je Mungu amekufanyia matendo gani makuu? Kwa nini ushuhuda wako kuhusu matendo makuu, ni muhimu sana?

**SIKU YA 238.**
**(Agosti 25)**

# Yesu amponya binti Yairo, na mama aliyeugua miaka 12.

**Marko 5.**



Yesu aliporudi chomboni na kujiandaa kuvuka ili arudi, watu wengi walikuwa wamekusanyika ng'ambo ya bahari. Akaja mtu mmoja katika wakuu wa sinagogi, jina lake Yairo, na akamwangukia miguuni Yesu; akimsihi sana, "binti yangu mdogo wa miaka 12 yu katika kufa, nakuomba uje uweke mkono wako juu yake, apate kupona na kuishi." Yesu akaenda pamoja naye, mkutano nao ukamfuata ukimsonga. Huyu mkuu wa sinagogi alikuwa ameondoa mawazo yote ya kumhukumu Yesu au kumsema vibaya kwani alikuwa na shida, na ingemsaidia nini angejidai 'kujua' au kwamba ni hodari wakati mambo yake yameharibika.

Watu wakiendelea kumsonga, akatokea mwanamke mmoja aliyekuwa ana ugonjwa wa kutoka damu miaka 12. Mwaka aliozaliwa mtoto wa Yairo ndiyo mwaka huyu mama huyu alianza kuugua. Hii ni miaka mingi, mtoto aweza kuzaliwa mpaka kufika darasa la saba, na bado huyu mama anaendelea kuugua. Alikuwa ameenda

kwa matabibu wengi na aliamua aguse pindo la vazi Lake kwa imani. Huenda matabibu hawa walimtoza pesa nyingi, na kumsumbua kwa vipimo au mambo mengi; na haikusaidia kupata nafuu. Aliishi maisha ya umaskini, maana alitoa fedha zake zote kwa matibabu. Hata leo tu ukiugua ni gharama kubwa kujiuguza. Mama huyu pia alitengwa kama sheria ya Musa ilivyoelekeza. Hakuweza kwenda kanisani, au ibada ya aina yoyote. Hakuweza kuwa na watoto au kuwa na wenzake kwa miaka 12. Alikuwa amepitia machungu mengi. Aliposikia Yesu anapita, na kwamba amesaidia wengi kuwaponya magonjwa ya mwili, na roho na hata kufufua wafu, aliamua naye ajikaze aende. Basi alipomwona Yesu alishikwa na woga akiogopa umati, maana alijua hakustahili kuwepo kwenye umati wa watu kutokana na ugonjwa wake. Hivyo badala ya kujipeleka mbele ili aonane na Yesu, aliamua aguse pindo la vazi la Yesu kwa imani. Papo hapo damu ile ilikauka na akafahamu kwamba amepona na msiba ule.

Yesu alifahamu nafsini mwake kilichotokea; kwamba kuna nguvu zimemtoka, akageuka akitazama mkutano na kusema "Ni nani amenigusa mavazi yangu." Wanafunzi wakashangaa na kumwambia, "umati wote huu unaokusonga, Wewe unauliza nani amekugusa?" Yesu akatazama pande zote ili aone, ni nani alimgusa, hapo ndipo yule mwanamke kwa hofu na kutetemeka, akijua lililompata akaja na kumwangukia Yesu na kumweleza kweli yote. Kulikuwa hakuna kuficha tena. Yesu akasema "Binti imani yako imekuponya, enenda zao kwa amani, uwe mzima, usiwe na msiba wako tena." Hata leo nasi, tuliguse pindo la vazi Lake, kwa maombi ya imani.

Yairo, mkuu wa sinagogi, aliendelea kumgoja Yesu akizungumza na mama mgonjwa, na wengine barabarani. Aliwaza mbona Mwalimu anachelewa sasa itakuwaje na nimemwambia binti yangu ni mgonjwa mahututi? Yesu hakufanya vitu kwa haraka, wala hatusomi mahali kwamba alikuwa na kawaida ya kwenda mbio. Alikuwa mtu mtulivu aliyeenda kutokana na maagizo toka kwa BABA wa mbinguni. Yairo akiwa anamngojea Yesu, watumishi kutoka nyumbani kwake wakaja na kumwambia "binti yako amekwisha kufa usimsumbue mwalimu." Baba wa watu, hakujua la kufanya, watu wakaanza kumpa pole; ila Yesu alikuwa amesikia na akamwambia "usiogope, amini tu." Naye akiwa amelemewa na mawazo, aliamua angojee tu.

Walipofika nyumbani kwa Yairo, Yesu Hakutaka wengi wamfuate isipokuwa Petro, Yakobo na Yohana ambao aliwaalika waende Naye kwenye nyumba ya Yairo. Yesu hakuvutiwa na mazingira yaliyokuwepo pale msibani. Kulikuwa na ghasia, watu wakilia, wengine kutokana na huzuni na wengine wakiwa wamekodishwa kwa kazi hiyo. Kukodisha watu wa kulia kulifanywa ili kuongeza sauti kubwa zaidi kwenye mazishi, ili pengine yule mtu aonekane alipendwa zaidi. Yesu akiona maombolezo makuu aliwaambia "mbona mnafanya ghasia na kulia, kijana hakufa, bali amelala tu." Wale watalaamu wa kifo, au wajuaji walifikiri mioyoni mwao, mtoto hana mapigo ya moyo, hapumui na pia hana msukumo wa damu (presha) anasemaje hajafa? Wakaangua kicheko sana, kumcheka Yesu, ndipo aliwatoa watu nje na kumtwaa baba mtoto, na mamaye pamoja na wanafunzi watatu na kuingia nao ndani ya chumba.

Akamshika yule mtoto wa miaka 12, ambaye mikono yake ilikuwa baridi na imepooza tayari kwani alikuwa amekishwa kufa, na akasema “Talita kumi” ikimaanisha msichana nakuambia inuka. Mara mtoto yule msichana akasimama na akaenda kwa mama yake, watu wakashangaa mshangao mkuu. Yesu akawaonya sana mtu asijue habari ile, kisha akaamuru mtoto apewe chakula. Wazazi wale hawakukaa kimya, waliwaambia ndugu zao, na marafiki zao, na kila mtu, habari zikaenea kila mahali, kukawa na furaha kuu. Hata leo Yesu anapenda watoto wadogo. Watoto msisite kumwuliza Yesu kile mnachohitaji leo. Jina zuri sana mtu kupewa, Talita! Jirani yangu wa nyumba inayofuatia yetu, ana binti ambaye anayesomea saikolojia Ureno, naye anaitwa Talita!

Yesu hakuogopa kukaa na wagonjwa, au watu ambao wanatisha. Wale ambao wamefanya kazi hospitalini watakubaliana nami jinsi magonjwa mengine yalivyokuwa ya kutisha, kwani vidonda vikiwa vikubwa huwa vinanuka. Magonjwa haya mtu akiwa nayo, hata jamaa wengine wanafunga pua kwa harufu za kuoza mwili, na kujaribu kumwepuka yule mtu. Yesu hakumwepuka mtu, au kuonyesha kuogopa kwenda karibu na watu hawa wenye shida. Alitumia fursa hii kuwasaidia wapate wokovu. Yesu alitambua kuwa mtu akiwa kwenye shida kubwa na hana wa kumsaidia, na watu wamemkimbia, anakuwa mnyenyekevu na rahisi kumwamini Mungu kuliko wakati mwingine.

Ni muhimu tukumbuke Mungu alivyotutoa kwenye mashimo ya shida kama hizi, katika siku za huko nyuma pale mambo yetu yanapoenda vizuri sana. Tusimsahau Mungu  na watu wengine wenye mahitaji.

*Kuishi kwa Neno la MUNGU kunamaanisha kusalimisha Kwake maisha yote. Kutakuwa na hisia ya kuendelea kuwa na uhitaji na utegemezi, kuuvuta moyo kumfuata MUNGU. Maombi ni lazima; kwani ni uhai wa roho. Maombi ya familia, maombi ya hadhara, yana nafasi yake; lakini ni ushirika wa siri na MUNGU ndiyo unaodumisha maisha ya roho.

-----------------------------------

Maswali: Yesu alimwambia nini Yairo, alipoambiwa binti yake ameshakufa? Yesu alimwambia msichana wa miaka 12 maneno gani? Je ugonjwa wa yule mama wa miaka 12 ulimpa masononeko gani? Je leo twawezaje kumgusa Yesu mguso wa imani? Talita ina maana gani?

**SIKU YA 239.**
**(Agosti 26)**

# Huwezi kutumikia mabwana wawili.

**Luka 16.**

Kisha Yesu akatoa mfano wa mtu aliyekuwa tajiri na alikuwa na wakili wake, huyu alishitakiwa kwake kuwa anatapanya mali zake baada ya mkaguzi wa mahesabu kuja. Bwana yule akamwita wakili, na akamwambia, ni habari gani hii ninayosikia juu yako? Toa hesabu ya uwakili wako, kwa kuwa huwezi kuwa wakili tena. Yule wakili alikuwa mjanja, naye akasema moyoni, nifanyeje maana bwana wangu ataniondoa kazi ya uwakili wa mali zake, nami kulima siwezi maana ni mvivu, na kuomba siwezi ni kujiabisha, basi najua nitakalotenda. Nitatumia hila ya kuwasaidia wanaodaiwa na tajiri wangu ili nitakapotolewa katika uwakili wanikaribishe nyumbani mwao ili kuepuka kuwa mtu asiye na kazi.

Akawaita wadeni wa bwana wake akianzia na wa kwanza akamwambia "una deni kiasi gani na bwana wangu?" yule bwana akamjibu "vipimo mia vya mafuta" akamwambia "twaa hati yako, na keti upesi, badilisha iwe hamsini tu." Kisha akamwambia mwingine una deni kiasi gani? Naye akasema makanda mia ya ngano, naye akamwambia, "twaa hati yako, na badilisha iwe themanini tu." Yule wakili dhalimu akaonekana mwerevu kwa kuwa alitumia busara ya dunia hii. Yesu anasema "wana wa ulimwengu huu huonekana wana 'akili' ambazo ni za utapeli kuliko wana wa Nuru."

Yesu akasema, hata nyinyi mjifanyie urafiki na Mungu kama huyu wakili mjanja alivyofanya, ili siku moja awakaribishe katika makao ya miele. Aliye mwaminifu kwa madogo sana huwa mwaminifu kwa makubwa. Mtu mfujaji mali ya watu hata ya Mungu ataifuja tu. Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili, kwani atamchukia huyu na kumpenda yule, ama atashikamana na huyu na kumdharu mwingine. Hatuwezi kumtumikia Mungu na mali, kwani mali ni mmiliki anayeendesha watu kupita chochote, na shina ya maovu yote ni kupenda mali. Wengi wamefikiri wakiwa na mali wataitumia kwa kazi ya Mungu, na kusaidia wenye mahitaji. Wamelaumu matajiri kwa kutumia mali vibaya, ila inapofika zamu yao kupata mali, wanatumia bila hekima wakipita mule mule walimopitia wale wengine waliowalaumu.

Muda wetu, talanta zetu, mivuto yetu, miili yetu na hata fedha au mali zetu, ni vya BWANA wetu, na sisi tu mawakili Wake tu. Tumekabidhiwa kutunza kwa uaminifu mengi ambayo si yetu. Endapo tutafikiri tulivyo navyo ni vyetu na twaweza kufanya tupendavyo, basi tunatumikia bwana mwingine, na si Mungu wa mbinguni. Basi mafarisayo waliopenda pesa waliposikia vile walianza kumdhihaki kwa sababu alikuwa maskini, akawaambia mnajidai haki mbele ya watu lakini Mungu awajua mioyo yenu; na lile mnaliona ni la muhimu sana kwenu Mungu halioni hivyo.
Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa

Mungu, hii yaonyesha sisi tupo katika familia ya Mungu. Paulo anasema ‘Kwa sababu hiyo nampigia magoti Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa Jina Lake jamaa yote ya mbinguni na duniani inaitwa.” Hivyo tumepewa tulivyo navyo ili tuvisimamie vyema kama wanafamilia, hili ni jukumu letu takatifu. Tuna hazina hata ile ya mbinguni, na hivyo tusiweke mioyo yetu kwa vitu vya kupita. Mbingu yote ilimiminwa kwaajili yetu, kwa Zawadi ya Mwana wa Pekee kuja kufa kwaajili yetu. Hebu tuwe wakarimu wa mali zetu kusaidia wengine na kusaidia kazi ya Mungu.
Akawaambia torati na manabii ndiyo Maandiko pekee yalikuwepo mpaka Yohana alipokuja ila kutoka hapo ufalme wa Mungu umehubiriwa kila mahali na watu wako tayari kuupokea. Basi mara zote tufanye yale tunayoagizwa na Mungu.

*Hakuna jambo lolote lile linalohusu mvurugiko wa amani mioyoni mwetu ambalo ni dogo sana Kwake Yeye kutambua. Hakuna sura katika uzoefu wa maisha yetu iliyo yenye giza mno Kwake Yeye kuisoma; hakuna mifadhaiko migumu sana Kwake kuweza kuiondoa. Uhusiano kati ya MUNGU na kila nafsi umetofautiana na umesheheni kana kwamba hakuna mwanadamu mwingine duniani ambaye amewahi kushiriki utunzaji Wake, ni kama vile hakuna mtu mwingine duniani ambaye kwaye alimtoa Mwanaye mpendwa isipokuwa mtu huyu mmoja tu.
-------------------------------

Maswali: Wakili mjanja alifanya maarifa gani? Kwa nini Yesu anasema tuwe wajanja kama wakili huyu? Kwa nini Mafarisayo waliopenda pesa walimchukia Yesu? Wakili ina maana gani? Mungu ametukabidhi tuwe mawakili wa mambo gani leo?

**SIKU YA 240.**
**(Agosti 27)**

# Mfano wa tajiri na Lazaro.

**Luka 16.**



Yesu akatoa mfano ambao mafarisayo walikuwa nao katika hadithi au hekaya za mapokeo yao akisema kulikuwa tajiri aliyevaa nguo za zambarau na kitani safi na ghali na kula siku zote vyakula ghali vya anasa. Na maskini mmoja aitwaye Lazaro, aliyekuwa na mazoea ya kukaa langoni pake tajiri, alikuwa ana vidonda vingi. Basi Lazaro alipata njaa na akatamani kushibishwa hata na makombo yaliyoanguka katika meza ya yule tajiri; wakati huo mbwa wakaja wakamramba vidonda vyake.

Basi ikawa siku moja yule maskini alikufa, akachukuliwa na malaika mpaka kifuani mwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa na kuzikwa. Basi yule tajiri kule kuzimu aliyainua macho yake alipokuwa katika mateso ya jehanamu akamwona Ibrahimu kwa mbali na Lazaro kifuani mwake. Tajiri akalia akisema "Ee baba Ibrahimu, nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake maji, auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu. Ibrahimu akasema "Mwanangu kumbuka ya kwamba wewe uliyapokea mambo mema katika maisha yako, na Lazaro

vivyo hivyo alipata mabaya hata nawe hukumsaidia; na sasa mambo yamegeuka naye yupo hapa paradiso anafarijiwa na wewe unaumizwa. Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumekuwa na shimo kubwa ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu.

Akasema baba nakuomba umtume nyumbani kwa baba yangu, kwa kuwa nina ndugu watano ambao wanaishi duniani bado hawajafa, ili awashuhudie wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso yaani Jehanamu. Ibrahimu akasema "wanao Musa na manabii, na wawasikilize wao." Tajiri akajibu, La! baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu. Akamwambia, wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishiwa hata na mtu aliyefufuka katika wafu.

Akawaambia mafarisayo waliopenda kisa hiki kwamba japo si cha kweli bali ni hekaya za mapokeo yao kwamba wenyewe wanasisitiza mtu asikie Maandiko na kuyatenda wakati anaishi, maana hakuna kubadilisha tabia baada ya kufa. Yale yanayotendwa katika maisha haya, huyaathiri maisha ya siku zijazo. Basi imempasa kila mtu kutilia makini kutenda mema, katika maisha h

aya asije kupata adhabu. Mfano huu unakiuka kanuni zingine za Maandiko au ufalme wa Mungu. Mfano huu ulikuwa mfano wa hekaya zao na si kisa halisi ambacho chaweza kutokea dhahiri au kiukweli. Hapa kwetu twafananisha na kile kisa cha sungura na mzee kobe, ambacho kilikuwa na mafundisho fulani, ila si kisa halisi.

Twasema hivi hasa kwa kuangalia mambo yanayotajwa, mfano; kifua cha Ibrahimu hakiwezi kuweka watu wote au hata mtu mmoja, maana hata Ibrahimu atapataje raha endapo watu wamemkalia kifuani pale mbinguni? Tena mtu aliye Jehanamu hana uwezo wa kuona yanayoendelea mbinguni. Hata hivyo fundisho tunalolipata hapa ni kuwa, zile huduma tunazozitenda kwa wenye mahitaji hapa duniani zina mshahara wake.

*Hakuna lugha inayoweza kuielezea, ni zaidi ya maarifa. Sisi ni wamoja na Kristo, maisha yetu yamefichwa pamoja na Kristo katika MUNGU. Tumehakikishiwa kwamba wakati Yeye ambaye ni maisha yetu atakapotokea, ndipo pia nasi tutatokea pamoja Naye katika utukufu. Kwa ujasiri mkubwa, tunaweza kumwita MUNGU Baba yetu.
----------------------------

Maswali: Kisa cha Lazaro na tajiri kinatufundisha nini? Kwa nini hili si tukio halisi bali hekaya? Je Mungu ametoa uzima wa milele kwa waovu?

**SIKU YA 241.**
**(Agosti 28)**

# Kurudisha shukrani.

**Luka 17**



Yesu alimponya mtu mwenye ukoma aliyemjia. Siku zile watu waliamini ukoma ni adhabu ya Mungu kwa mtu aliyefanya dhambi. Hii ilikuwa dhana potofu. Watu waliougua ukoma kama adhabu ambao wametajwa kwenye Biblia ni wachache tu kama mfalme Uzia na Miriamu, dada wa Musa. Mkoma anayetajwa hapa aliendа na wengine bahari ya Galilaya. Huenda alijificha na kuchunguza huku na huku kujiridhisha kama watu hawamuoni. Bila hivyo ingekuwa vigumu kumfikia Yesu, maana watu wangemzuia. Mwishowe alisema potelea mbali akaenda karibu na Yesu mbele ya ule umati, japo wengine walimtolea maneno, kisha alianguka chini na kumsihi Yesu "BWANA kama unataka nitakase." Yesu alinyosha mkono Wake kwa mkoma huyu, kiasi ambacho yule mkoma alishangazwa maana kwa muda wote huo, hakuna aliyemgusa kwa mikono Yake. Akamwambia aende kwa kuhani amkague, kama Sheria ya Musa inavyoagiza, ili aweze kurudi kwa jamii bila kutengwa. Mtu huyu alieleza yote yaliyotokea. Makuhani wengine walifurahi na kuona kuwa hizo ni habari njema ila wengine walikuwa na chuki na ghadhabu.

Ikawa siku nyingine, katika juma la mateso alipokuwa njiani kuelekea Yerusalemu alipita katika kijiji cha Samaria, akaona watu kumi wengine wenye ukoma waliokuwa wamesimama kwa mbali kwani walihesabiwa najisi, na hawakuruhusiwa kuwa karibu na watu. Ilibidi wapaze sauti zao wakisema "najisi, najisi" huku wakipita, ili kuwatahadharisha watu wawakimbie. Watu hawa walifukuzwa, na kutengwa na watu kwa kuogopa wasiwaambukize. Wengine waliishi kwenye mapango wakiwa hawana mahitaji, kwa kuwa wametengwa mbali na watu. Watu hawa kumi walipaza sauti "Ee Yesu BWANA mkubwa uturehemu." Alipowaona aliwaambia, Enendeni mkajionyeshe kwa makuhani. Huu ulikuwa ni utaratibu kwa mujibu wa sheria ya Musa. Ikawa walipokuwa wanaenda njiani wakajiona wamepona. Mmoja wao alipoona amepona alirudi kutoa shukurani, akimtukuza Mungu kwa sauti kuu, akaanguka kifudifudi miguuni pa Yesu akamshukuru, naye alikuwa mtu wa mataifa na Msamaria.

Yesu akamwuliza yule Msamaria "Je wale wengine hawakutakaswa au kupona ukoma?" Yule Msamaria akajibu "wametakaswa", na Yesu akauliza "wako wapi wale tisa basi, hakuna aliyerudi, kumpa Mungu utukufu isipokuwa mgeni huyu?" Basi alimwambia yule Msamaria aende akimwambia "Imani yako imekuokoa."Wale wengine walioponywa hawakuwa na sababu za msingi za kutokurudi na kushukru. Wengine walisema kwamba wataenda siku nyingine kutoa shukurani, wengine wakaona wangoje kwanza waone kama wamepona kweli, na udhuru mwingine mwingi ulio hafifu ulitolewa. Tunachojifunza kuhusu ugonjwa wa ukoma ni kuwa ugonjwa huu ulikuwa wa kutisha mno, maana sehemu za mwili kama mikono, pua, masikio, miguu, vidole huoza na kulika pole pole mwishowe hudondoka na kutoweka. Hisia za mwili kama maumivu hutoweka, na mtu anaweza kuungua moto bila kujua. Maumivu ya mwili mara nyingi ni msaada, kwani ni yowe ambalo mwili unapiga kuonyesha shida inayoendelea ili turekebishe au tuepuke, mfano kama tumegusa kitu cha moto au tindikali, tunatoa mkono haraka ili tusijiumize.

Watu waliokuwa na ugonjwa huu hawakuweza kuishi na jamii zao. Walipiga makelele ya tahadhari ili kuwaandaa watu wasiwaguse watakapokuwa wakipita. Watu wote walitoka njiani ili kuwapisha. Waliishi katika nyumba zao wenyewe bila kuchangamana na watu kwa kuwa walikuwa wametengwa. Jamii iliwaletea chakula na kuweka mbali ili wasikutane na kugusana kuepuka maambukizi, maana siku zile dawa ya ukoma ilikuwa haijagundulika. Mtu mwenye watoto, mke au mume alitengwa asiishi na jamii yake. Maisha yalikuwa ya huzuni, ila watu hawa tisa, walidiriki kutokuwa na shukrani. Wengine huenda waliingiliwa na kiburi cha kutokubali kwamba wamesaidiwa. Wengi hata siku hizi hawataki msaada, kwa kuhofia wasije wakaonekana ni dhaifu kwa kuwa wamesaidiwa. Hili ni kosa, kwenye ufalme wa Mungu. Watu wanapaswa kusaidiana na kupeana shukrani. Tukishukuru kwa kusema asante, wengine wanaiga mfano wetu, na kushukuru pia.

Yesu akasema mfano "Je ni nani kati yetu ambaye mwenye mtumishi, alimaye au achungaye ng'ombe, atakayemwambia mara arudipo toka shambani, njoo ule mimi nimeshakutayarishia chakula? Je hatamwambia yule mtumishi japo amechoka na kazi "nifanyie tayari chakula, nile, jifunge ukatumike hata niishe kula na kunywa ndipo nawe utakapokula na kunywa? Je atampa asante yule mtumwa kwa sababu

amefanya aliyoagizwa? Vivyo hivyo nanyi mtakapokwisha kuyafanya yote mliyoagizwa semeni “sisi tu watumwa wasio na faida; tumefanya tu yaliyotupasa kufanya”

Miujiza ni mambo yatokeayo kwa jinsi ya ajabu isiyo ya kawaida, kwa asili. Miujiza si uchawi. Uchawi unatumika kuumiza watu, na kwa nguvu za Ibilisi au giza. Yesu alitumia nguvu Zake kuponywa wagonjwa, kulisha wenye njaa na kumtoa Shetani ndani ya watu. Miujiza Yake haikuonyesha tu Yeye ni Mwana wa Mungu, bali upendo mkuu aliokuwa na huruma aliyokuwa nayo kwetu binadamu ambao tumejeruhiwa na mwovu. Biblia inatuambia tunapokuwa wagonjwa tuombe, tumwone daktari na kutumia tiba rahisi, na Mungu atatuponya. Wakati mwingine Mungu katika hekima Yake anaona kwamba ni vyema mtu asipone haraka, au asipone kabisa.

Timotheo alikuwa na tatizo la tumbo, na akapata msaada tiba rahisi kwa kunywa maji ya mizabibu. Lakini Paulo alipokuwa na shida ya mwili wake aliambiwa hataweza kupona, na kwamba atamtukuza Mungu zaidi katika huo udhaifu wake. Mungu alimpa Paulo nguvu za kustahimili udhaifu au maumivu haya. Mungu anataka mema tu kwetu. Katika ile picha kubwa ya wokovu au kuokolewa kwetu “Mungu Hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani wale walioitwa kwa kusudi Lake.” Kwa kawaida kupona ni jambo ‘jema’ ambalo Mungu ameahidi kututendea tunapomwomba. Lakini hata kama hatutapona papo hapo, bado tumtumaini Mungu, kwamba anatupenda na Yeye aweza kutumia hata ugonjwa kwa ajili ya ‘mema’ kwetu. Siku moja maovu na mabaya yote yatakoma katika maisha yetu, na maisha yetu yatajaa furaha na uwepo wa Mungu.
*Mahali pa Kukimbilia Ambapo pako wazi Sikuzote — Njia ya kuendea kwenye kiti cha enzi cha MUNGU iko wazi kila wakati. Hauwezi kupiga magoti kila wakati kwa ajili ya maombi, lakini maombi yako ya kimya yanaweza kuendelea kupaa juu kwa MUNGU kila wakati kwa ajili ya kuwezeshwa na kuongozwa. Utakapojaribiwa, kama itakavyokuwa, unaweza kukimbilia mahali pa siri pa Aliye Juu. Mikono yake ya milele itakuwa chini yako.
--------------------------

Maswali: Je waweza kutoa sababu saba walizotoa wenye ukoma waliponywa ila hawakurudi kutoa shukurani? Kwa nini wenye ukoma hawakuishi na watu?

**SIKU YA 242.**
**(Agosti 29)**

# Dhambi yaweza kumfuata mtu kanisani.

**Luka 18 na 21.**

Yesu akawambia imewapasa kumwomba Mungu siku zote wala wasikate tamaa. Maana Mungu atawapatia haki na kujibu wale wanaomlilia usiku na mchana. Ila Je atakapokuja Mwana-Adamu yaani Yesu Mwenyewe, Je atakuta watu wakiwa na imani duniani? Au wamejisahau na maisha na kukata tamaa? Yesu alikutana na watu waliopenda kujiona wapo juu na kujifanya wao wana dini sana, au kujiona kuwa dini yao ilikuwa bora kuliko wengine. Siku zile watoza ushuru walionekana ni wasaliti, na wengi wao walikuwa wezi wa pesa za watu kwa kutoza pesa kubwa na kuweka mifukoni mwao. Watoza ushuru wengi walikuwa matajiri na watu waliwachukia.

Yesu akatoa mfano wa watu wawili, walioenda hekaluni kusali, mmoja Farisayo na na mwingine mtoza ushuru. Mafarisayo walikuwa wanajiona ni wenye haki, na kuwahesabu wengine kuwa wenye dhambi. Mtoza ushuru yeye alijijua ni mwenye dhambi. Wakiwa wanasali hekaluni Farisayo alisimama akijisifu akisema, "Eh Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi wadhalimu, wazinzi, na kama huyu mtoza ushuru. Mimi nafunga mara mbili kwa juma; hutoa zaka katika mapato yangu yote. Mtu huyu alisahau anazungumza na Mungu, na si kujisifia kwa Mungu, si kuwasengenya watu kwa Mungu, kujilinganisha au kuchunguza mambo ya watu wengine. Yule mtoza ushuru, yeye alisimama mbali na mimbari wala hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipiga piga kifuani akisema "Eh Mungu nisamehe mimi mwenye dhambi."

Yesu akasema mtoza ushuru aliendа nyumbani kwake akiwa amehesabiwa haki kuliko yule Farisayo, maana yule Farisayo alijikweza na kujisifu, na kwa hiyo atashuswa na yule mtoza ushuru aliyejishusha atakwezwa. Maombi si kuwasengenya watu wa Mungu, bali ni kuzungumza na Mungu kama rafiki yetu. Hata leo ukitaka Mungu akusikilize usimpashe habari jinsi ulivyo mwema na wengine walivyo wabaya, maana Yeye anakujua fika. Wewe shughulika na kumwambia shida yako ni nini, na kwamba unahitaji msaada Wake. Wale wanaomtegemea Mungu na kukiri wamekosa, watapewa uzima wa milele. Ni makosa kufikiria kwamba tu wema kuliko wengine, na kwamba hatukosei chochote ila wengine ndiyo wana shida. Tusiwadharau wengine kwamba wana dhambi kutushinda kwani Yesu anawapenda wao pia, na alikufa kwa ajili yao.

Yesu akiwa hekaluni siku moja, wakati wa kuhitimisha huduma yake duniani, aliona jambo ambalo limebariki mamilioni ya watu duniani. Wenye pesa na matajiri wakienda kutoa sadaka kubwa kubwa, zisizotoa sauti, ambazo ni mabaki tu ya matumizi yao ya nyumbani. Akaja mjane maskini, akatembea pole pole kwa woga, mpaka kwenye kisanduku cha sadaka na kutoa sadaka yake. Yesu alitambua

ukarimu wa mwanamke yule ambaye hakutaka kujigamba, wala kujionyesha kwamba ametoa kiasi gani. Alijua pia kile alichobakiza nyumbani! Akawaambia wale wanaomsikiliza "Mmemwona yule mjane? Hakika nawambia huyu mjane maskini ametoa sakaka kuliko wote. Maana hao wote walitia sadaka katika mali iliyowazidi bali huyu katika umaskini wake, ametia vyote alivyokuwa navyo."

Huenda mama huyu aliambiwa na wenzake ya kwamba yeye ni maskini sana, kwa nini ajisumbue kutoa pesa zake zote alizo nazo? Si abaki tu na ile pesa? Waweza hata leo kuambiwa na marafiki, wazazi au walimu wako hivyo hivyo. Ila usikubali kukosa baraka kama Roho wa Mungu anakutuma utoe. Hakuna aliyetoa kwa Mungu akawa maskini. Mama huyu aliamini Mungu alitaka asaidie kazi Yake. Machozi ya furaha yalimtoka, akafarijika moyoni Yesu alipotoa maneno ya kupongeza tendo alilofanya. Zawadi yake ni kumbukumbu ya vizazi vyote, kwamba alijitoa pengine hata kukosa chakula, ili apate hizo senti mbili, akiamini Mungu atamtunza na kumsaidia katika mahitaji yake yote.

Mama huyu pia ni mfano kwa wale wanaosema kwamba hawatoi sadaka maana kuna watu  wezi  kule kanisani, nao watazichukua zile pesa! Badala yake Yesu alimpongeza na kusema amefanya vyema, wala hakusema kwamba asitoe, japo alijua mama huyu ni masikini, na pia aliwajua mafarisayo walikuwa wanafiki na wabaradhifu wa mali za wajane!

Hata leo wajane na yatima wapo na wengine ni maskini sana. Wajane hao wanatakiwa kumpa Mungu shukrani kwa kutoa mioyo yao kwa upendo kwake. Zawadi zetu ndogo tunazotoa kwa mioyo mikunjufu kwa Yesu, huzizidisha, zikawa mifereji ya za thamani kubwa. Yesu abariki ile roho na nia tunayotoa nayo. Japo kile tunachotoa ni kidogo Yeye hukizidisha ili kubariki wengi.  Watu wametoa mamilioni ya dola, kwa sababu ya sadaka ya mjane huyu, aliyoleta kwenye hazina. Moyo wa mama huyu masikini wa kujitoa umegusa mamilioni ya watu, katika kila nchi.

Hakuna awezaye kujua thamani kamili ya sadaka zetu zilizotolewa kwa utukufu wa Mungu na upendo zinavyoweza kubariki kazi ya Mungu na mahitaji ya wenye shida. Zawezwa kuwa mwangwi unaovuma milele. Tukumbuke Mungu humbariki mtoaji hata kama kwa upande mwingine watenda kazi wa kanisa hutumia pesa hizo kwa mambo yao binafsi. Usiache kutoa sadaka kwa sababu unadhani kuna wezi wanaoiba hizo sadaka. Hata hivyo kila mtu ana wajibu kufanya sehemu yake, sehemu yako ni kutoa, na sehemu ya mwenzako ni kutunza kilichotolewa na kukitumia kwa malengo yaliyokusudiwa. Usipate hofu kwamba kuna watu wabaradhifu wa zaka na sadaka, fanya utafiti na ukigundua kuna wizi katika kanisa ambalo linaongozwa na Maandiko, zungumza na uongozi au chukua hatua zinazofaa kuwaelezea, ila usiache kutoa Zaka na Sadaka kwaajili ya watu waovu. Yesu alijua baadhi ya makuhani na mafarisayo walikuwa matapeli, ila hakumwambia mjane wa senti mbili kwamba usilete pesa yako humu kanisani, kwani kuna matapeli wataojinufaisha matumbo yao! Badala yake, alimpongeza, akimaanisha kwamba ule wizi wa uongozi usimfanye mtoaji kutomrudishia Baba wa mbinguni sehemu ya Baraka Zake, ili atupe Neema tele!

Mjane wa senti mbili, hakuwa na mawazo kwamba huenda senti mbili hizi zitaliwa, hata kama zitatumiwa nje ya malengo yaliyokusudiwa si hoja yake yeye, sehemu yake amefanya na wajibu wake ametimiza. Nawe timiza wajibu wako kwa Mungu wako. Na kila mmoja atafanya sehemu yake.

*Siri ya Nguvu za Kiroho-Maombi ni pumzi ya roho. Ni siri ya nguvu za kiroho. Hakuna njia nyingine ya neema inayoweza kuwa mbadala na halafu afya ya roho ikawa salama. Ombi huupatia moyo mawasiliano ya haraka na Chemchemi ya uzima, na kuimarisha mishipa na misuli ya uzoefu wa kidini. Puuzia zoezi la sala, au jihusishe na maombi bila mpangilio mara hapa, au pale kama unavyoona inafaa kwako, nawe utafanya mkono wako upoteze kumshikilia MUNGU. Nguvu za kiroho hupoteza ukali wake, na uzoefu wa kidini hukosa afya na nguvu.

-----------------

Kwanini Yesu alimpongeza mjane aliyetoa senti mbili? Kwanini tutoe sadaka?

**SIKU YA 243.**
**(Agosti 30)**

# Zakayo mtu mfupi apanda mti.

**Luka 19**



Yesu Akasema "imewapasa kumwomba Mungu siku zote, wala msikate tamaa. Akatoa mfano wa hakimu katika mji fulani, ambaye hakumcha Mungu wala kujali watu. Na katika mji huo kulikuwa na mjane aliyekuwa akimwendea endea mara nyingi akimwomba amsaidie apate haki na adui yake. Naye yule hakimu alikataa kwa muda yale maombi ya mjane. Alipoendelea kufuatwa fuatwa, akanuia moyoni mwake kumwondoa huyu mama msumbufu "japo simjali Mungu au watu, lakini kwa kuwa mjane huyu ananiudhi, nitampatia haki yake, asije akanichosha kwa kunijia daima. Yesu akasema sikilizeni asemavyo yule kadhi dhalimu, Mungu Je hatawapatia haki wateule Wake wanaomlilia usiku na mchana naye, Je Yeye si bora kuliko yule hakimu kusikia vilio vya watu Wake wanaomwomba."

Aliwaambia mfano huo watu walio na kiburi huku wakijidhania kuwa kila wanachofanya kipo sawa na kuwaona wengine hawafai. Aliwatahadharisha wamkumbuke mke wa Lutu aliyegeuka kuwa nguzo ya chumvi. Yesu alitoa mfano mwingine wa mtu aliyejiwa na wageni usiku na akaenda kuomba mkate kwa jirani

yake. Yesu alitoa mifano ikawafanya watu wawe na shauku ya kumwabudu Mungu. Aliondoa pazia, na kuta zilizowatenga watu. Kwa miujiza hii watu wakaona tabia ya Mungu, na kujua upendo wake. Waliondoa nadharia kwamba Mungu anasubiri wafanye mabaya ili awaadhibu. Awaambie nimekupata sasa! Hivyo sivyo Mungu wetu alivyo.

Yesu aliwaonyesha ile Kweli ya Mungu ilivyo, na jinsi ilivyojaa upendo, uvumilivu, urafiki, huruma na haki. Yesu alizungumza kuhusu ufalme wa Mungu kwamba hakuna kiovu kitakachoruhusiwa kule, na kila mtu atakayeingia ni yule atakayemwamini. Wale wanaomwamini Yesu wanagundua kwamba watakuwa na furaha, na wataondolewa hofu walizo nazo, kwa vile Mungu anajali maslahi yao. Watu walijawa na hasira na uovu, kwa kuwa waliwachukia watu wasitake kuwasamehe.

Yesu hakuponya wenye magonjwa na pepo tu, bali hata wenye ugonjwa wa tamaa za vitu na mali. Tunahitaji kujazwa na Roho Mtakatifu, na si 'roho mtakavitu!'. Yesu akaingia Yeriko, alipita katikati ya mji, na tazama palikuwa na mtu aitwaye Zakayo, mkubwa mmoja katika watoza ushuru, ambaye ni tajiri. Huyu aliposikia Yesu anakuja kwenye mji anamoishi, alitamani sana amwone, ila umati ulikuwa mkubwa naye alikuwa mfupi wa kimo hata asiweze kumuona. Mji huu wa biashara ulikuwa maili 25 kutoka Yerusalemu, na ulijaa watu mashuhuri kama wafanya biashara, maofisa wa Kirumi, na makuhani.

Zakayo akatangulia mbele alipopata habari kwamba Yesu atapita njia ile. Watu walivyomchukia wasingemruhusu akae mbele, ila hakukatishwa tamaa. Alikuwa na nia na mpango aliopanga kichwani, na bila aibu tajiri mashuhuri mwenye nguo za gharama, mtu huyu mzima alipanda mti wa mkuyu ili apate kumwona Yesu atakapopita njia ile. Hii ilikuwa mojawapo ya burudani au mkanda ambao watu wa Yeriko waliona siku ile na kucheka. Basi Akakaa katika panda zuri la mti, akichungulia chini, na huku akijiuliza, Je Huyu Ndiye Yesu, au ni Yule kule? Alichokuwa akitamani kukipata ilikuwa ni kumwona Yesu, na wala hakufikiri zaidi ya hapo.

Lazima alikuwa ameanza kumpenda Mungu, na hata aliposikia Mathayo naye mtoza ushuru amepewa nafasi ya kufanya kazi na Yesu, alijipa moyo zaidi. Yesu alipofika pale kwenye ule mti alitazama juu, macho yao yakakutana. Zakayo akashangaa maana hakutegemea kabisa tukio hilo. Alikuwa ameweka juhudi zake katika kumtambua Yesu kwenye ule umati, na ghafla akashangaa wanatazamana uso kwa uso na Yesu. Msafara wote ukamtazama mtu wamjuaye kama mpenda pesa, na mwovu. Yesu akamwambia "Zakayo shuka upesi" kwa kuwa imenipasa leo kushinda nyumbani mwako. Zakayo yaweza kuwa aliangalia kama kuna mtu mwingine ana jina lile, na akauliza "ni mimi?" akijisonda. Akaona amebarikiwa kiasi gani kwamba kwenye umati ule wa maelfu waliomfuata Yesu, ni kwake tu Zakayo ndiko ambako Yesu alijialika, na wala si kwa mwingine.

Hatujui kwa nini Yesu alisema afanye upesi. Yesu hakukaa masaa machache tu bali alishinda, siku nzima! Ukiwa wa Zakayo wote ukamtoka, maana Yesu alimpa haja za moyo wake yaani zile haja halisi, zilizompa Zakayo huzuni. Zakayo hakuwa yule Zakayo wa kawaida tena. Maisha yake yote yalibadilika. Sijui Kwa nini Yesu

alimwambia ashuke upesi. Jambo la kushangaza ni kuwa Zakayo alitii. Hakuwa na kiburi, kwani alishuka haraka haraka, na akamkaribisha kwa furaha nyumbani mwake. Huenda alichafua meza na mapochopocho maana alikuwa na mali nyingi. Moyoni akitabasamu alifikiri, "hata jina langu Yesu analijua jamani?" Je ingekuwa wewe ungemkaribishaje Yesu siku hiyo?"

Watu wengine walinung'unika walipoona hayo, wakisema "ameingia kukaa kwa mtu mwenye dhambi." Wakiwa sebuleni, wakizungumza na Yesu, alijua amewakwaza wengi, na Roho wa Mungu akampa hekima, akasimama mbele ya Yesu, kuonyesha msisitizo na kusema "BWANA, tazama nusu ya mali yangu yote nitawapa masikini, na ikiwa nimemnyang'anya mtu kitu, kwa hila namrudishia mara nne." Japo watu waliomsikia walifikiri hizi ni porojo tu, ila Yesu aliyeutambua moyo wa Zakayo, alitambua kuwa Zakayo hakuwa anafanya porojo. Alijua Zakayo ameongoka, na anampenda Mungu. Toba ya kweli ni pamoja na kujenga pale tulipobomoa. Yesu anatoa neema tuweze kusahihisha pale tulipoharibu.

Yesu akamwambia Zakayo kwa furaha "Leo wokovu umefika nyumbani humu, kwa sababu huyu naye ni mwana wa Ibrahimu." Yesu akasema Maneno mazito ambayo leo twapasa tujipe moyo nayo, na kila siku tuyarudie "Mwana wa Mungu, na Mwana wa Adamu, alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea." Mungu alimkubali Zakayo kama mtoto wake. Mimi na wewe tumepotea, Mungu anatutafuta leo. Hitaji Lake kubwa ni kumwokoa mwanadamu. Twaweza kuwa tumepotea kiroho tukiwa nyumbani, kanisani au shuleni, lakini kwa kuwa anatupenda, Masihi bado anatutafuta. Zakayo hakusahau siku hii maishani mwake.
Watoza ushuru hawakupendwa na watu maana walidhaniwa kuwa ni wezi, na wasaliti wa Wayahudi mana walikusanya kodi kwa niaba ya himaya ya Rumi. Watoza ushuru waliwauliza wafanya biashara mali walizo nazo, kisha wakawatwanga kwa kodi kubwa, ile ya halali wakarudisha kwa serikali na nyingine wakaweka kibindoni. Zakayo alikuwa na cheo kikubwa kwenye kazi hii. Alikuwa na wengi chini yake waliotoza ushuru. Alikuwa tajiri mkuu aliyejulikana. Alikuwa na nyumba nzuri, mashamba, mifugo na nguvu, ila alikuwa hana furaha.

Maana hata ukiwa tajiri sana, zile mali peke yake haziwezi kukuletea furaha. Kila mtu huvaa jozi ya kiatu kimoja tu, hata awe tajiri kiasi gani. Kila mtu hulala kwenye kitanda kimoja tu hata awe tajiri. Kila mtu hula chakula cha kawaida tu, iwe mahindi, matunda, mboga, nyama au samaki. Watu matajiri hawawezi kula dhahabu eti kwa kuwa wao ni matajiri. Hivyo matajiri hufadhaika na vile vitu vingi na mali nyingi kwa kuwa huwa zinawapa utupu wa namna fulani maishani. Matumizi ya pesa ni matatu tu, kila mahali duniani; nayo ni mahitaji yetu, mahitaji ya wenye shida na mahitaji ya kueneza kazi ya Mungu. Mahitaji yetu yakiwa yamekidhiwa, basi ni rahisi kutumia pesa kuondoa ukiwa au utupu tukifikiri itatupa ucheshi; ila pesa haiwezi kufanya vile kila siku. Ni Yesu tu anayeweza kuleta furaha na kuondoa ukiwa, akitusaidia kutupa maana ya kuishi na jinsi ya kuishi bila dhamira kutushitaki.

Toba ya kweli lazima iwe na mabadiliko kwenye maisha yetu ya kila siku. Biashara zetu lazima zimpe Mungu utukufu, na zisiwe za kuwaibia watu na kuwalaghai. Je tunauza vitu vyetu kwa bei ya kuumiza au kudhulumu watu? Je, tunawaambia watu

wapunguze chini sana bei za bidhaa zao, na hivyo tupate kuwadhulumu, wakati wana uwezo mdogo kuliko sisi? Hata siku hizi mashirika ya kukusanya kodi yana watu kama Zakayo wanaodhulumu watu na kujichukulia pesa, tabia hii ni mbaya na dhuluma kwa mwanadamu. Wengi hufikiri kwamba shida hii po Afrika tu!, la! Shida hii ipo kila alipo binadamu duniani! Zakayo anatupa mfano mzuri wa toba ya kweli, yaani kuweka sawa mambo na wale tuliowaumiza, na pia kutoa mali yetu itumike kueneza injili, ili watu wengi wafike mbinguni siku moja. Japo aliruhusiwa na Warumi kujiwekea pesa zingine zaidi ya kodi, bado alijua tendo hilo ni kosa ndiyo maana alitubu. Basi sisi nasi tumwombe Mungu toba ya kweli, iliyo halisi na inayolenga na kulingana na kile tulichokosea, tukitaje kama kilivyo. Yaani tuseme tulichokosea, tutubu, na tumwombe atupe njia ya kusahihisha au kuacha.
Zakayo anatuonyesha japo kuwa ni vigumu kwa tajiri kuingia mbinguni, neema ya Yesu yabadilisha watu matajiri, waokolewe. Yesu anamtafuta kila mtu leo. Je, wewe upo tayari kutembea Naye na kufanya urafiki Naye leo?

*Usipuuzie maombi ya siri, kwa maana ni moyo w mambo ya kiroho. Kwa maombi ya dhati, ya bidii omba usafi wa roho. Omba kwa bidii, kwa shauku, na kwa dhati, kama ambavyo ungeliomba endapo maisha yako yangekuwa hatarini. Endeleakubakia hapo kwenye uwepo wake kumtumainia MUNGU mpaka matamanio ambayo hayawezi kutamkika yatakapozaliwa ndani yako kwa ajili ya wokovu, na ushahidi mzuri wa dhambi zilizosamehewa umepatikana.
-------------------------

Maswali: Kwa nini watu walimchukia Zakayo? Kwa nini Zakayo aliamua kwenda kumwona Yesu? Zakayo alijuaje wale aliowadhulumu ili awarudishie alichowaibia? Yesu alisema Maneno gani makuu kwenye nyumba ya Zakayo?

**SIKU YA 244.**
**(Agosti 31)**

# Imani ya mwanamke mkakanayo.

**Mathayo 15**



Yesu akaulizwa na Mafarisayo na Waandishi wa sheria kwa nini wanafunzi Wake wanaharibu mapokeo ya wazee kwa kutonawa mikono kabla ya kula? Akawaambia wao wako tayari kutunza mapokeo ya binadamu bali huvunja sheria za Mungu bila kujali. Akawapa mfano wa amri ya tano inayosema "Waheshimu baba yako na mama" Lakini wao wasipotaka kuwasaidia wazazi wao na mali zao, husema kitu hiki "nimekiweka wakfu" kusudi tu asimsaidie mzazi wake. Akawaambia huo ni unafiki, maana wanamheshimu Mungu kwa midomo yao tu, ila mioyo yao i mbali, maana walifundisha mafundisho na mapokeo ya binadamu. Hata leo watu wengi huchukua mapokeo ya dini zao na kuacha Neno la Mungu. Hili ni kosa kubwa. Kisha akawaambia "si kitu kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi maana chenyewe chaenda chooni, bali kimtokacho mtu kinywani chaonyesha moyo wake umejaa nini." Alimaanisha kwamba Wayahudi walikuwa wanajali kunawa mikono ili wasile vitu vichafu, wakati maneno yao yanayotoka midomoni yalikuwa ni maovu. Ikiwa watu wanayo mawazo maovu kama wizi, uongo, uuaji, hiyo ni shida kubwa zaidi ya kutonawa mikono. Wanafunzi walimwambia "mafarisayo wamechukia Ile

Kweli." Naye aliwaambia chochote "Baba Yangu asichokipanda kitang'olewa." Na akawaonya kuhusu mafarisayo, kwamba ni vipofu, na viongozi wa vipofu, na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, wote watatumbukia shimoni.

Yesu akaenda miji ya Sidoni na Tiro, karibu na bahari ya Mediteranian. Hapa watu waliabudu miungu mingine. Huko ilikuwa nchi nyingine kabisa, kama vile mtu aende Ethiopia au Msumbiji. Hapa mitume waliona kwamba kwa kuwa wapo nje ya Uyahudi, watakuwa na nafasi ya kutulia na kuzungumza na mwalimu wao; na tazama mwanamke Myunani, kabila lake ni Msirofoinike akamjia, akampazia sauti akisema "unirehemu BWANA mwana wa Daudi, binti yangu amepagawa na pepo" umsaidie. Ila Yesu hakujibu akitaka kumpa mtihani na kuwafundisha wanafunzi wake ambao alipanga wachukue injili kwa mataifa yote duniani, na ya kwamba wasiwe na ubaguzi. Nao wanafunzi wakiona Yesu amekaa kimya walimwambia, amwache na aende zake, maana kelele zake zimezidi hata alikuwa ameanza kuudhi watu. Walifikiri kwa kupendekeza mwanamke yule atimuliwe wangemfurahisha Yesu kwa vile ambavyo alikuwa anabugudhiwa na mtu asiyestahili wa kabila au nchi ngeni. Isitoshe huyu mama alikuwa mtu wa dini ya kipagani au makafiri.

Wakashangaa Yesu alipowaambia, hakutumwa kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli peke yake bali kwa kila binadamu. Wokovu ni kama jua; binadamu wote wanapaswa wamulikiwe ili wachague wenyewe kupokea wokovu au kupotea. Basi yule mama alikuja na kumsujudia, akisema "BWANA nisaidie" maana binti yake alikuwa anaumwa, akahitaji huruma na uponyaji toka kwa Yesu kama binadamu mwingine yoyote; maana kwa Mungu wote tuko sawa. Yesu huugua pale ambapo yeyote kati yetu huwa na shida, awe Mrundi, Mnyarwanda, Mgogo, Msukuma, Mkisii, Mmayote, Mjaluo, Muacholi, Mkongomani, Mhabeshi au Msomali. Ndipo Yesu akajibu "si vyema kukitwaa chakula cha watoto na kumtupia mbwa." Akiwa na maana watu wa mataifa nje ya Israeli ni mbwa. Mama hakukasirika, akajibu kwa hekima ya kutamanika toka mbinguni.

Tuelewe kwamba maandishi hayawezi kutueleza sauti ya Yesu au uso wa tabasamu kwa huyu mama alipozungumza, hivyo mara zingine tunafikiri yalikuwa maneno machungu kwa mtu aliyemwumba; ila huyu mama alipoona uso wa Yesu na sauti Yake, akaona ana baraka za kupata kile alichokiomba bila mashaka na akasema "Ndiyo BWANA lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao." Ni nani leo asingependa kuwa mbwa wa mfalme wa wafalme? Japo sisi tu binadamu wala hatuwezi kufananishwa na mbwa, mama huyu alijua, kuwa mbwa wa Mwana wa Daudi ni bora kuliko vitu vya wafalme wa dunia hii.

Wengi pale ninapoishi leo wanaelewa zaidi hili kwani wanapenda mbwa mno. Hawa wana vitanda vizuri kwa ajili ya mbwa, wana chakula rasmi kwa mbwa, na hata wengine wanabusu mbwa na kuwafanya kama watoto wao wa kuzaa. Jirani yangu mmoja aliniambia anatumia dola 1,000 kila mwezi kulisha mbwa wake aliyekuwa na kilo 140. Mwingine aliniambia alitumia maelfu ya dola mbwa wake apate kufanyiwa upasuaji wa figo, na mbwa akapona. Wengi kule Afrika wasingeweza kumudu matibabu hayo na huenda wangeamua kununua mbwa mwingine. Watu husema mbwa ni rafiki asiyeacha kupenda mtu na, wala hana kinyongo. Kwa vile

watu wengi huishi peke yao, mbwa amekuwa msaada kwao kwa ukiwa na hata kusaidia kuongoza vipofu kutembea, au kujilinda na wezi.

Magharibi yathamini mbwa. Ila enzi zile, na hata siku hizi watu wana ukatili kwa mbwa pale wanapowaumiza kwa kuwapiga kwa mawe bila kosa. Mbwa ni wanyama ambao ni viumbe vya Mungu na tukumbuke wana maisha ya shida kwa ajili ya dhambi yetu binadamu. Japo Yesu hakufa kwa ajili ya mbwa, na binadamu ana thamani zaidi ya mbwa; hata hivyo tukiwa kama Balaamu na kutosikia maagizo Yake, basi hata punda au mbwa watakuwa msaada kwa watu kuliko sisi. Mungu anapenda viumbe Vyake vyote. Ni bora kuwa wanyama wanaotii kama punda wa Baalamu. Mwanamke huyu alijua Yesu ni Mwana wa Daudi na akamkiri. Ndipo Yesu akajibu "mama imani yako ni kubwa, na iwe kwako utakavyo." Binti yake akapona saa ile ile nyumbani alipokuwa amelala kitandani. Pepo lile baya lililomtesa likamwondoka.

Japo Yesu alitumwa kwanza kwa Wayahudi, anampenda kila mtu kutoka sehemu yoyote. Sisi sote tu watoto Wake. Inawezekana tukafikiri maneno yake yalikuwa ya kuudhi kwa yule mama, ila alitaka wanafunzi wajifunze jinsi thamani ya roho ya kila kabila, jamaa, lugha na nchi ilivyo. Yesu alitaka kumsaidia alipotokeza tu. Je wewe unafikiri kabila lako ni bora kuliko la wengine? Au mama yako ndiye mzuri kuliko wengine wote duniani? Yawezekana kuna ukweli ila kwa Mungu sote tuko sawa. Hajali wapi unatoka, anachojali ni kuwa amekuumba na ana mpango na wewe. Mwanamke huyu na majirani zake, waliohudumiwa, hawakubaki walivyo, bali walimwamini Mungu.

Yesu akaondoka kule Sidoni na Tiro na kwenda kando ya bahari ya Galilaya na kuketi mlimani, na makutano wengi wakamletea vipofu, mabubu, vilema na wengine wenye shida, akawaponya na wengi wakamtukuza Mungu wa Israeli. Akamwona mtu kiziwi, asiyeweza kuzungumza, akamchukua kando faragha na kutia vidole vyake masikioni, kisha akatema mate na kumgusa ulimi, kisha akatazama juu mbinguni akiugua, akamwambia 'efatha' maana yake funguka. Mara masikio yake yakafunguka, na ulimi wake ukalegea akaweza kuongea. Akawaonya wasimwambie mtu, ila alivyowaambia ndiyo walivyozidi kusambaza habari hizi. Watu wote walishangaa mno wakisema "ametenda mambo yote vyema, viziwi awafanya wasikie, na bubu waseme."

Ila moyo una magonjwa ya kufisha, na ni mdanganyifu, ni nani aweza kuujua? Ingawa Yesu alimponya kila aliyemwomba, na hawakuhitaji kutumia fedha kama malipo ya matibabu; bado viongozi wa makuhani walitaka kumwua. Siku hizi matabibu ambao ni mabingwa wa upasuaji wanatoza pesa kubwa sana, kama dola 50,000 au mamilioni ya shilingi kwa upasuaji mmoja. Hapa alikuwepo Yeye anayetibu bila kutoza gharama. Hapa palikuwa na tabibu ambaye hakuacha kidonda au maumivu bila kutoa huduma, Tabibu ambaye hakuhitaji kulaza watu kwa miezi kadhaa hospitalini, au kufanya upasuaji, au kuwaambia wanunue dawa na bado watu walikuwa na hila za kumwua.

Yesu alifanya miujiza takribani 37 iliyorekodiwa kwenye Biblia. Vijiji vingi

alipotembelea, hakuacha hata mgonjwa mmoja, wote waliomjia waliponywa. Alifanya miujiza mingi. Yaonekana alichukua muda kuponya watu na kusikiliza shida zao, zaidi ya kuhubiri. Miujiza Yake ilionyesha wazi kwamba ana uwezo hata kwa nguvu za asili. Alipoukemea upepo, au kutembea juu ya maji ni udhihirisho wa uwezo wake juu ya vitu vya asili. Alionyesha ana uwezo juu ya magonjwa, uwezo juu ya mapepo wachafu au Shetani, na zaidi ya yote uwezo juu ya kifo chenyewe. Hakuna lililo gumu Kwake YEYE. Yesu anatupenda wewe na mimi, na ana uwezo wote, tusisahau hilo kamwe, na hata tukiwa na tatizo lolote, liwe dogo au kubwa tusisite kumwambia.

Mungu anafurahi ukimwambia fadhaa na furaha zako na anapenda sana kuleta ufumbuzi wa kukufaa mno, kuliko unavyoweza kujihudumia mwenyewe. Mkabidhi Fadhaa zako zote, na Mwambie "Nitakwenda" Nawe kufanya utumishi Wako (Mathayo 29:19-20)

*Kwa Jina Langu," Kristo aliwaamuru wanafunzi Wake waombe. katika Jina la Kristo wafuasi wake wanapaswa kusimama mbele za MUNGU. Kupitia thamani ya kafara iliyotolewa kwa ajili yao, wana thamani machoni pa Bwana. Kwa sababu ya haki kupitia Kristo wanahesabiwa kuwa wa thamani. Kwa ajili ya Kristo, Bwana huwasamehe wale wamchao. Haoni ubaya wa mwenye dhambi ndani yao. Anatambua mfano wa Mwanawe ndani yao, ambaye wanamuamini.
---------------------------

Maswali: Ni kitu gani kimtiacho unajisi mtu? "mbwa hula makombo yaangukayo mezani mwa bwana zao" ina maana gani? Je Yesu ana uwezo wa mambo gani? alivyozidi kuwaambia watu wasiseme kuhusu mwujiza ndiyo walivyozidi kusema, Kwa nini walifanya vile? Yesu alifanya miujiza mingapi?

**SIKU YA 245.**
**(Septemba 1)**

# Kulishwa kwa watu 4000 mikate na samaki mara ya pili.

**Marko 7-9**



Akiendelea kuponya watu Dekapolisi, pale ambapo aliwaagiza wale wenye pepo wawili wagerasi au Gadara waende wakashuhudie na kuwa wamishonari huko. Mkutano ulikuwa mkubwa maana walikaa kwa siku tatu, nao walikuwa wamekosa chakula; walichoka na njaa na hata wengine kuzidiwa na kulegea sana. Wanafunzi wakatoa mawazo kwamba mkutano ufungwe na makutano hao waruhusiwa warudi makwao maana hawana kitu cha kuwalisha, hata kama kingekuwapo kisingewatosha maana walikuwa wengi mno.

Yesu akawaita wanafunzi Wake na kuwaambia kwa upendo "nawahurumia makutano kwa sababu yapata siku tatu wamekaa nami, wala hawana kitu cha kula, nami nikiwaaga waende zao nyumbani kwao hali wamefunga sipendi kwani watazimia njiani na baadhi yao wametoka mbali." Wanafunzi wakiwa wamesahau uwezo wa Yesu, au pengine walifikiria Yesu hatafanya muujiza wa kuwapa chakula watu wasio

Wayahudi, wakajibu watapataje mikate ya kushibisha watu wote hawa nyikani? Akawauliza wao wana mikate mingapi hapo walipo, maana ulicho nacho mkononi ukiwa tayari kukitoa ndicho Yesu atatumia kusaidia watu. Wakamwambia kuna mikate saba, na visamaki vichache. Akaitwaa ile mikate na visamaki, akashukuru na kuvimega na kuwapa wanafunzi Wake, nao wanafunzi wakawapa makutano.

Hapa tunajifunza kushukuru kwa Mwenyezi Mungu ni jambo muhimu, tusile kama ndege walavyo. Sisi tuna utashi wa kujua ni BWANA anatupa mkate au riziki yetu yoyote kila siku, "ni jambo Jema kumshukuru BWANA na kuliimbia Jina Lake." Wote wakala na kushiba na wakaokota masazo ya vikapu saba vimejaa, nao waliokula walikuwa wanaume elfu nne, wanawake na watoto. Akapanda chomboni akaenda Dalmanutha. Wakatoka mafarisayo wakaanza kuhojiana Naye wakitaka ishara itokayo mbinguni wakimjaribu, Naye akasikitika rohoni Mwake, akisema "kizazi hiki chatafuta ishara, hakitapewa ishara kwani walikuwa wameona na kusikia yote ya kujenga imani na kufanya maamuzi ila mioyo yao ilikuwa migumu.

Akapanda chomboni na kwenda Zake. Yesu alielewa kwamba kwa miaka zaidi ya miwili ametembea na kufanya miujiza mingi. Wanafunzi Wake waliijua miujiza hiyo maana hakuifanyia sirini, bali Shetani aliwafunga, wasiamini. Maneno ya Yesu kwa wale waliomwamini, yalibadilisha maisha ya wengi. Kuanzia kuzaliwa kwa Yesu kwa njia ya ajabu, nyota zilizowaongoza watu angani, malaika walioimba, na mambo mengine yote waliyapuuzia. Yesu alisikitika kwamba wanataka tu aendelee kuwaonyesha miujiza mingine, na akajua hiyo haitawasaidia kuwafanya wamwamini Mungu.

Akawaambia ishara ya Yona ndiyo tu imewabakia, maana hata Ninawi watu waliokolewa kwa vile walikuwa tayari kumsikia Mungu na kumkubali, ila Wayahudi hawakutaka kuwa wanyenyekevu. Watu hawa waliona miujiza mingi ya waliopona, ila hawakujali. Watu waliokuwa na maamivu, nao walitaka ishara zao, na hata hizo wangeziona Yesu alijua hazingewasaidia kuamini, maana walifanya mioyo yao kuwa migumu. Japo wanafunzi wao wangependa mwalimu wao aonyeshe maajabu zaidi wakifikiri itafanya watu watamkubali, Yesu alijua mioyo yao wote. Hata leo kuna wengine wanaobadilisha Maandiko kama mafarisayo, wakijitafutia kujikidhi haja zao kwa mafundisho makuu fulani. Hawa kama mafarisayo, wangetaka kuonekana wao ni mashuhuri na wenye uwezo pale mahali walipo.

Shida ya watu wengi ni ubinafsi na umimi, au kutojali huduma ya Yesu aliyoitoa kwetu. Wayahudi hawakuelewa kwa vile hawakutaka kuelewa. Wao waliona matendo yao ya nje au kazi wanazomfanyia Mungu ndiyo muhimu. Mungu anaona maisha yetu, tunavyoishi, ndiyo muhimu kwanza, ndipo yale matendo yetu. Hata leo kazi zetu nzuri tunazomfanyia Yesu, zaweza kuharibiwa kwa kujipenda wenyewe. Kukazania mapokeo ya binadamu yasiyo kwenye Maandiko au sheria za Mungu ni kujipenda. Mungu tu Ndiye aweza kutubadilisha nia zetu binadamu tusiwe wa kujifikiria wenyewe zaidi ya wenzetu. Badiliko hili la Moyo ni muujiza mkubwa kupita yote, na ishara ya kweli kwamba Mungu anafanya kazi katika maisha yetu. Maisha ya Yesu yalikuwa mwujiza na ishara kubwa kati yao, nao wakapuuzia. Alifanya kazi za Mwenyezi Mungu aliyemtuma, na kuzungumza kweli ya Maneno

ya Mungu. Hata leo kuna wengi wanataka muujiza ili waamini kama Mungu yupo, na Mungu akijua kweli hilo litasaidia, atawapa muujiza. Lakini kama ni kupata muujiza tu, ili tufurahi na kushangaa, kama tuko katika mchezo wa mazingaombwe, haitasaidia maisha yetu sasa. Wengi siku hizi tunataka nasi tuone miujiza inayofanana na ile Yesu aliyotenda au ile ya manabii ili tupime na kuamini, kama Mungu anajali maisha yetu. Cha kuamua ni kwamba, maisha ya mtu yakibadilika kutoka kuwa mbinafsi asiyependa watu na kuwa mkarimu anayependa kuhudumia watu, huo ni muujiza wa peke yake. Muujiza huu wa moyo mgumu wa binadamu kubadilika, unaonyesha Mungu yupo. Pale ambapo Neno la Mungu linahubiriwa, Roho Wa Mungu hufanya ishara na miujiza kubadilisha maisha ya watu, waanze kuishi kuelekea uzimani.

Yesu akafika Bethsaida na wakamletea kipofu wakisihi amguse kumponya; Naye akamshika na kumchukua nje ya kijiji, akamtemea mate machoni, akamwekea mikono Yake, akamwuliza kama anaona kitu. Yule kipofu akasema "naona watu kama miti inakwenda." Ndipo akaweka mikono Yake juu ya macho yake, naye akatazama sana na akawa mzima, akiona yote wazi wazi. Wakatoka na kwenda chomboni, mitume wakajikuta wana mkate mmoja tu, wamesahau mingine. Yesu akasema "Jihadharini na chachu ya mafarisayo na Herodi." Wanafunzi wakafikiri anazungumza kuhusu mikate waliyosahau, wakaanza kubishana pengine "ni wewe ndiye uliyesahau."

Yesu akatambua na kusema mbona mnabishana sababu hamna mikate, hamjafahamu ninayozungumzia? Mbona mioyo yenu ni mizito kuelewa "mna macho hamwoni, mna masikio hamsikii, mna ubongo wala hamkumbuki. Akawauliza yaliyotokea kwenye kuwapa mikate watu mara ya kwanza, na safari hii ya pili, bado wakawa hawajaelewa. Yesu alizungumza chachu ya mafarisayo akimaanisha mafundisho ya imani ya uongo, yaliyo na ujanja ujanja au walakini. Akachukua wanafunzi Wake kwenda Kaisaria Filipi na njiani akawauliza wanafunzi Wake "Watu huninena mimi ni nani? Wakamjibu wengine husema Yesu ni Yohana mbatizaji, wengine Yeremia au Eliya na wengine mojawapo wa manabii.

Naye akawauliza wao" na Nyinyi mnasema ya kuwa Mimi ni nani? Wakamwambia "Wewe Ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Akamwambia Petro Simoni Bayona, mwili na damu hakukufunulia hili bali Baba Yangu wa mbinguni. Nami nakwambia wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa Langu; wala milango ya kuzimu halitalishinda. Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni. Na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni." Akawaonya wasimwambie mtu.

Akawaambia mara ya pili kuhusu kifo Chake "imempasa Mwana wa Adamu kupatikana na mateso mengi na kukataliwa na wazee, wakuu wa makuhani, na waandishi, kisha kuuawa na baada ya siku tatu kufufuka. Naye akiwa ananena hivyo wazi wazi mbele ya wanafunzi Wake, Petro alimchukua faragha na kuanza kumkemea kwamba haya hayatampata yeye, akifikiri anafanya jambo jema. Ulipita muda mfupi tu, alikuwa amemmkiri Yesu kama Masihi, ila haikupita hata siku

akaanza kutumiwa na Shetani. Ndipo Yesu akijua Shetani anamtumia mwanafunzi Wake, bila mwanafunzi kujua, akageuka na akawatazama wanafunzi Wake, na kumkemea Petro akisema “Nenda nyuma Yangu Shetani, maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu.”

Basi inabidi kujihadhari mara nyingi tunenapo. Twaweza kufikiri ni maneno mazuri tu ya kumtia nguvu au faraja mwenzetu na kumbe ni kinyume cha Maandiko. Maandiko yalisema Masihi lazima apitie yale, kinyume cha hivyo ni kupinga kazi ya Mungu.

*Ikiwa hauhisi hatari yoyote, na ikiwa hautoi maombi ya kusihi msaada na nguvu za kupinga vishawishi, hakika utapotea; kupuuza kwako wajibu kutaandikwa katika kitabu cha MUNGU mbinguni, na utakutwa umepunguka katika siku ile ya hukumu.
---------------------------

Maswali: Watu wangapi walilishwa? Petro alikuwa alitumiwaje na Shetani? Ishara gani wangeiamini Wayahudi? Chachu ya mafarisayo ni ipi? Yesu alimponyaje kipofu?

**SIKU YA 246.**
**(Septemba 2)**

# Kubeba msalaba na kukana nafsi.

**Marko 8, Mathayo 17**



Akawaita mkutano pamoja na wanafunzi Wake akawaambia "mtu yoyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe na ajitwike msalaba wake na anifuate, kwa kuwa mtu anayetaka kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili Yangu na kwa ajili ya injili, huyo ataisalimisha. Akawaambia itamfaidia nini mtu akipata ulimwengu wote unaokaa muda mfupi tu na nafsi yake au kupoteza uzima wa milele. Akawaambia wakimwonea haya BWANA na maneno Yake katika kizazi cha dhambi, basi hata Yeye atawaonea haya atakapokuja katika utukufu wa Baba Yake pamoja na malaika watakatifu. Akasema kila binadamu siku ya mwisho ya hukumu atalipwa kwa kadiri ya matendo yake.

Akawaambia wanafunzi Wake kwamba kuna watu ambao hawatakufa mpaka watakapouona ufalme wa mbinguni umekuja kwa nguvu, akimaanisha kuonekana kwa utukufu au mng'ao wa Yesu. Hata baada ya siku sita, Yesu aliwatwaa Petro, Yakobo na Yohana na kuwaleta juu ya mlima mrefu faraghani, akageuka sura Yake mbele yao, sura Yake ikawa na utukufu na mwanga wa nguvu. Mavazi Yake yakameta meta, yakawa meupe mno asivyoweza dobi wa duniani kuyafanya meupe. Wakatokea Eliya na Musa walioishi duniani na walio mbinguni sasa, kuja kumtia faraja na nguvu, kabla ya kifo Chake. Petro, Yakobo na Yohana wasingeweza kuwajua, ila Yesu aliwatambulisha kisha waliwasikia katika mazungumzo yaliyoendelea.

Hawa walikuwa wameishi kama wanadamu wakajua vile moyo Wake ulivyokuwa na huzuni. Kama Yesu angeshindwa kumaliza kazi Yake ya kutoa kafara, hata hawa mbingu isingekuwa yao tena, maana walitangulia kwenda mbinguni kwa kafara au neema ya kile ambacho Yesu angeenda kukifanya msalabani siku chache zinazokuja. Eliya na Musa wakizungumza na Yesu, wanafunzi walikuwa wamelala wasipate mazungumzo yote, wangekuwa macho wangesaidiwa hata nguvu katika siku zinazokuja ili wasikimbie na kupungukiwa na imani. Petro alipoamka tu, asijue la kusema kwa mshangao na hofu nyingi alitoa wazo "Rabi ni vizuri sisi kuwapo hapa; na tufanye vibanda vitatu, kimoja chako wewe, kimoja cha Musa na kimoja

cha Eliya'. Hapo hapo likatokea wingu na kuwatia kivuli, na sauti ikatoka kwenye lile wingu ikisema "Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu, msikieni Yeye." Sauti hii kwenye Maandiko, ilisikika mara tatu, pale Yesu alibatizwa, Pale Yesu alikuwa na Wagiriki kwenye ua wa hekalu na hapa.

Wakatazama huku na kule ila hawakuona mtu wakaanguka kifuli fuli kwa woga. Ilikuwa sauti ya Mwenyezi Mungu toka mbinguni. Walipoanza kushuka mlimani aliwakataza wasimweleze mtu waliyoyaona hata afufuke katika wafu. Wakafanya vile ila walikuwa wakiulizana wao kwa wao "Ni nini maana ya kufufuka katika wafu." Wakamwuliza mbona waandishi wa mafarisayo husema kwamba Masihi hatakuja mpaka Eliya aje? Naye akawajibu kwamba Eliya anapaswa kuja kwanza kurejesha upya kwa kuwafanya watu wapate toba ya kweli ili kujitayarisha kwa kuja Masihi. Akaambiwa Eliya alishakuja, nao wakagundua ni Yohana mbatizaji na waovu walimtenda walivyotaka wakamtesa na kumwua.

Akawaambia pamoja na hayo Mwana Adamu atateswa sana na kudhararuliwa. Mitume wasijue haya ya kuteswa nao yanawangoja, baadaye walikumbuka Yesu alivyowaambia wasijisahau wakiwaamini makuhani maana ni mbwa wa mwitu walio ndani ya ngozi ya kondoo na watawapeleka mahakamani na kuwapiga mijeledi, nao wawe wajanja kama nyoka ila waaminifu na tabia njema kama hua. Mitume walitangatanga wasiwe na kikao, na wakapata dhiki kubwa, ila Yesu alikuwa amewaonya mbeleni. Hata sisi leo, tumeonywa na Maandiko, tuyasome ili mambo yasije kutufikia kwa ghafla tukaharibikiwa na kushindwa kuingia mbinguni. Yesu Yu mlangoni, anakaribia kuja sana! Pia mateso yaja, kwa wale wanaompenda Mungu ila Yesu ameahidi kutupa nguvu na msaada.

Kutembea safari ya dunia, ni majaliwa makubwa, Musa alitembea miaka 120 akiwaongoza wana wa Israeli kwa dhiki kuu maana walikuwa na mioyo migumu. Eliya naye akatembea miaka 700 baada ya Musa, yeye aliishi wakati Israeli iliabudu miungu mingi ya ajabu, yeye hakufa bali alitwaliwa mbinguni. Mitume nao wakikaa pale kwenye mlima na kushangaa shangaa walikuwa duniani wakisafiri, na wangeendelea kwa taabu baada ya Yesu kufa. Yesu alibarikiwa kusikia sauti ya BABA Yake, ndiyo maana hakupoteza muda kuwahakikishia Yeye ni nani, au kwa nini anatoa ishara kwao. Hakuwa na haja ya kuwahakikishia Yeye ni Mwana wa Mungu, alijua Yeye ni nani na BABA Yake alishamhakikishia na kumfariji. Hata leo ukiwa unafanya mapenzi ya Mungu na unaheshimu na kupenda watu, usijali utakaposemwa vibaya au kusingiziwa, hilo ni jambo la kawaida kabisa, watu wanaweza kukukalia vikao wakuseme au wakusute usoni, au hata wakuchangie kukupiga kwa pamoja, wewe mwelekezee Mungu shida zako. Kila binadamu anapitia safari hizo. Nami pia nimezipita mara kadhaa kwenye masimango, kejeli, dharau na mengineyo. Kama kwetu bado kuna amani na uhuru wa dini bado, tunapaswa kumshukuru Mungu kwa dhati, kwa ulinzi, wema na fadhili Zake.

Hata leo mtoto huna haja ya kuhakikishia watu kwamba umeumbwa na Mungu Naye ni BABA yako. Watu wakiwa wanakuuliza, ukijua wewe ni mtoto wa Mungu, na ni nani, hutakuwa na hofu bali utajitahidi umpendeze Mungu na kutafuta faraja ya Mungu zaidi ya watu. Maana watu hubadilika badilika, hata wale wa karibu

yetu, ila Mungu habadiliki, ni Yule Yule, jana, leo na hata milele. Mwenye Mamlaka ya mwisho na anayejua kila kitu ni Mungu, binadamu wengine sote sisi ni watu wa kupita, ni wasafiri, hivyo hatuwezi kuwa majaji wa thamani ya mtu, La! Mtu anaishi muda mfupi, hata akiwa na kazi nzuri, huwa anastaafu na mwishowe kufariki, Thamani yetu i ndani ya Mungu, Ndiye Mweza yote, na wa milele mbele na nyuma. Kile Mungu hawezi ni kutenda dhambi tu! Na hakuna ambaye anataka hilo!
*Maombi ni kuufungua moyo kwa MUNGU kama tuufunguavyo kwa rafiki. Jicho la imani litamtambua MUNGU aliye karibu sana, na mwombaji anaweza kupata ushahidi wa thamani wa upendo wa Mungu na kujali Kwake.


--------------------------------------------

Maswali: Je waweza kujitwika msalaba wako kwa namna gani? Yesu alionekanaje kwenye ule mlima? Kwa nini unafikiri Eliya na Musa walitumwa kwa Yesu? Kwa nini Petro alitaka kujenga vibanda vitatu? Kwa nini ni kosa kutokesha na kuomba kama Petro alivyofanya? Je, unaweza kufikiri sababu ya Musa kufurahi kuikanyaga nchi ya Kanani alipokuwa mlimani na Yesu?

**SIKU YA 247**
**(Septemba 3)**

# Wanafunzi washindwa kutoa pepo.

**Marko 9, Mathayo 17**



Makutano ya watu waliwafikia wanafunzi tisa waliobaki chini yaani bondeni, kusaidia kutoa mtu pepo, wakati Yesu na mitume watatu walikuwa kwenye mlima ambao Yesu alibadilika na utukufu wa mng'ao. Makutano hayo ya watu wakawa wakizungumza na waandishi wa mafarisayo wakijadiliana nao. Kisha mkutano wote ukashangaa walipomwona Yesu akitokezea na wakapiga mbio wakamfikia na kumsalimu. Yesu akawauliza wanajadiliana nini? Na mtu mmoja kwenye mkutano akajibu "Mwalimu nimemleta mwanangu kwao, ana pepo bubu, na kila anapompagaa, humbwaga chini, naye hutoka povu na kusaga meno na kukonda, nikaomba wanafunzi Wako wamtoe pepo wasiweze." Wanafunzi walikuwa na madhaifu kama ya leo. Walikuwa katika mjadala wa somo walilolipenda, la kupata cheo. Huko ni kukaa bondeni, leo tunataka tuwe mlimani kama Yesu ili tupate uzoefu Wake!

Mara nyingine walitumia Jina la Yesu kutoa pepo au kuponya magonjwa, wakitaka karama hiyo iwe yao tu, ingawa wengine walifanya kwa imani ya Yesu na walikuwa waumini wa kweli wenye nia ya kusaidia wengi! Walitumwa waende nje kama wale wanafunzi 70 waliweza kufanya maajabu, ila sasa walipojaribu kusaidia mtu kuponya wakashindwa. Walijaribu tena na tena wakashindwa, wakaona aibu na watu wakawa wakiwaangalia. Ndipo waligundua kwamba kuna kitu kinapungua kwao. Pengine waliona, ni afadhali hata wale ambao si mitume wa Yesu walikuwa bora siku ile kuliko wao. Mitume wakashangaa ni nini kimekuwa tofauti leo, mbona ule uwezo umewatoka? Somo ni nani mkuu kupita wote, hata leo linaleta taabu.

Wanafunzi walifikiria jinsi watakavyokuwa mawaziri kwenye ufalme wa Yesu, na kupata nguvu, uwezo, mali au mamlaka. Hata Yesu alipokuwa anawaambia kwamba anaenda kuuwawa, hawakuelewa, wakachanganyikiwa "Je anaamanisha kile anachokisema au ni fumbo", Yesu alizidi kukazia akiwakumbusha kuhusu kifo Chake tena na tena. Akawakumbusha yeye anayetaka kuwa wa kwanza

atakuwa wa mwisho na wa mwisho atakuwa wa kwanza. Akawaambia Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa bali kutumikia watu na kutoa maisha yake kuwaokoa wanadamu. Wanafunzi walipenda kusikia jinsi watakavyokuwa na vyeo, na jinsi watu watakavyowatumikia. Ila Yesu aliwaambia walihitaji kuwa watumishi na siyo mabwana. Wengi siku hizi twafikiri tukiwa mabosi basi Mungu ametubariki, na tukiwa watumwa Mungu ametulaani. Mara nyingi hili si kweli, kwani tuliona Yusufu alipokuwa gerezani bado BWANA alikuwa naye.

Baba ya mtoto akahuzunika, na ndipo Yesu akatokeza. Watu wakamkimbilia wakijua atafanya hili tena kwa urahisi. Basi Yesu kwa kusikitika alisema "Enyi kizazi kisichoamini, nikae nanyi hata lini? Mleteni kwangu." Wakamleta Kwake, na hata alipomwona, yule pepo akamtia kifafa naye akaanguka chini, akagaa gaa akitokwa na povu. Akamwuliza baba yake, amepatwa na hii shida toka lini? Akasema toka utoto, na pepo amemtupa motoni na katika maji ili amwangamize "Lakini ukiweza neno lolote tuhurumie, na kutusaidia." Yesu akasema unasema "ukiweza? Yote yawezekana kwaye aaminiye Mungu." Masikini huyu baba hakujua ni nani alikuwa akizungumza naye! Alikuwa akimwambia Bwana Yesu kwamba ukiweza mponye tafadhali! Masikini hakujua hapa alikuwa Yule ambaye Ndiye UZIMA wa MILELE! Ndipo yule baba wa kijana akalia kwa sauti akisema "Naamini, nisaidie kutoamini kwangu, au "naomba unipe imani." Tukiomba ombi la baba huyu tuko salama kabisa na tuendelee kujenga imani yetu, kwa kulisikia Neno la Mungu na kulipima na kulitenda. Imani huja kwa kusikia, kusikia Neno la Mungu. Na kulisoma pia, kama unajua kusoma, yote ni muhimu, napolisikia napata kitu, napolisoma napata kitu kingine ambacho kiliponyoka kwenye kusikia! Kila mtu amepewa kipimo cha imani. Hakuna mwanadamu chini ya jua asiye na imani. Tunalala tukiamini tutaamka, tunakaa kwenye kiti tukiamini hakitatudondosha! Tunaamimi maelfu ya mambo, hebu leo tuamini kwamba Mwenyezi Mungu ni Bwana wa maisha yetu, Naye anatupenda na Anao uwezo wote kuyabadilisha maisha yetu na kutusaidia kumpenda Yeye kwa mioyo yetu yote, nguvu zetu zote, akili zetu zote na roho zetu zote na kumtii na kumtumaini na kumtegemea!

Imba huu wimbo:

**KUMTEGEMEA MWOKOZI**

1. Kumtegemea Mwokozi, Kwangu tamu kabisa,
Kukubali neno lake, Nina raha moyoni.
    Yesu,Yesu namwamini, Nimemwona thabiti;
    Yesu,Yesu,yu thamani, Ahadi zake kweli.

2. Kumtegemea Mwokozi, Kwangu tamu kabisa,
Kuamini damu yake, Nimeoshwa kamili.

3. Kumtegemea Mwokozi, Kwangu tamu kabisa,
Kwake daima Napata, Uzima na amani.

4. Nafurahi kwa sababu, Nimekutegemea,
Yesu,Mpendwa na Rafiki, Uwe nami dawamu.

Hili ni ombi kila mmoja wetu apaswa kuliomba, na Mungu hawezi kusema hapana, kamwe, kamwe narudia hawezi, maana ni Mungu atakaye tuwe na imani. Yesu akaona mkusanyiko mkubwa ukikutanika kwa kasi, akamkemea yule pepo mchafu akamwambia “Ewe pepo bubu na kiziwi, nakuamuru umtoke huyu mtu na usimwingine tena.” Akalia na akamtia kifafa sana yule mtoto, akamtoka naye akawa kama amekufa. Watu wakadhani amekufa, ila Yesu alimshika mkono na kumwinua, akasimama amepona. Walipobaki wenyewe nyumbani, wanafunzi wake walimwuliza kwa faragha, mbona sisi hatukuweza kumtoa? Akawaambia pepo la namna hii haliwezi kutoka, isipokuwa kwa kuomba na kufunga, kwani uwezo wa kuponya, au kutoa mapepo au uwezo wa lolote lile jema watoka kwa Mungu. Nao walishangaa jinsi ule uwezo ulivyokosekana kwao. Leo ukizidiwa na lolote lile ambalo ni gumu, iwe ni masomo, umasikini, ugonjwa, ada, mazingira hatarishi, huzuni, kifo, mahusiano na mapepo, Mwite Yeye haraka! Atakusaidia kila tatizo lako, Omba, Omba, Omba!

Yesu aliwaambia kwamba mapepo yaweza kutolewa na kisha yakatoka, kama wakimtumaini na kumtegemea Mungu, maana Ndiye atoaye uwezo. Akawaambia wawe na maombi ya dhati na kufunga ili mambo haya magumu yawezekane. Akawakumbusha wasifikiri ni wao wenye uwezo wa kuyatoa bali ni YEYE. Ndipo akawaambia kama wakiwa na imani inayofanana na punje ya haradali tu, wangehamisha milima. Kuhamisha milima hakuna maana ya kuhamisha mlima Kilimanjaro hapa na pale kila wakati; bali ni kufanya tofauti kwa mambo makubwa au miujiza ili kusaidia wengine au kuhubiri Neno la Mungu. Hatuwezi kupewa imani, tusipoiomba. Lazima tuombe kwa Mungu. Yeye anajali uchaguzi na uhuru wetu, na hatulazimishi kutupatia imani. Basi tumwombe atuongezee imani yetu, maana itatusaidia tuishi maisha ya furaha, uaminifu na kuweza kuwaambia wengine matendo yake makuu. Hapa tunaona kwamba imani, maombi, na kufunga ni mojawapo ya silaha zinazohusika katika pambano kuu kati ya Shetani na Mungu na kuleta matokeo chanya kwenye maombi yetu.

Wakatoka wakaenda Galilaya asitake mtu yeyote ajue, ila akawaambia kwa mara ya tatu kuhusu kifo Chake “Mwana wa Adamu yuaenda kutiwa mikononi mwa watu nao watamwua, hata akiisha kuuwawa, baada ya siku tatu atafufuka.” Bado hawakufahamu alichowaambia, ila waliogopa kuuliza.

*Sala ni uhai wa roho — Maombi ni muhimu; kwani ni uhai wa roho. Maombi ya familia, maombi ya hadhara, haya yana nafasi yake; lakini ni ushirika wetu binafsi wa siri na MUNGU ndio unaodumisha maisha ya roho.

--------------------------

Maswali: Watu walimkimbilia Yesu akitoka wapi? Kwa nini wanafunzi walishindwa kumponya mtoto? Kwa nini uongozi wa kanisa au serikali una hatari kubwa? Tunawezaje kuepuka hatari za uongozi? Kwa nini “Nisaidie kutoamini kwangu” inapaswa kuwa ombi la kila binadamu leo? Mtoto huyu alikuwa ana pepo la aina gani?

**SIKU YA 248.**
**(Septemba 4)**

# Ni nani mkubwa katika ufalme wa Mungu.

**Marko 9**



Wakafika Kapernamu, akawauliza walishindania nini njiani, nao wakiona aibu wakanyamaza kwa maana njiani walikuwa wakibishana wao kwa wao kuhusu ni nani aliye mkubwa au bosi. Wanafunzi walipenda mada hii ya kupanda cheo, au kuwa watawala wakubwa. Ndipo, Yesu akaketi chini, akawaita wale thenashara yaani kumi na mbili na kuwaambia atakayekuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho kuliko wote, na mtumishi wa wote. Hakuwakataza kuchukua madaraka na kuwa wakubwa ila aliwaambia kwa kanuni ya mbinguni kiongozi ni mtumishi wa watu. Uongozi au madaraka ni hatari na majaribu makubwa kwa wengi. Huleta kiburi na kuanza kuwatesa watu au kuwadharau badala ya kuwasaidia katika shida zao, na kuwaongoza ili waweze kupata msaada.

Ni rahisi kuona kwamba tukiwa viongozi tutakuwa bora kuliko yule kiongozi tunayemwona sasa. Ila uongozi ni mtihani au jaribu kubwa linalowaangusha wengi dhambini. Wengi hufikiri uongozi wa serikali tu ndiyo wenye shida, ila tukiangalia katika historia uongozi wa makuhani au wachungaji ulikuwa una mpasuko pia,

kuliko uongozi wa Warumi au wa dunia. Hili ni fundisho kwetu tupatao kazi kanisani. Yesu hakupinga mtu kuwa kiongozi, bali alisema kiongozi anayempenda Mungu, sharti awe mtu wa kutumikia na kupenda watu, akiwatakia mema, na si kujishibisha tumbo lake tu, au maisha yake binafsi. Yesu alimwona mtoto mdogo kwenye umati amebebwa na mama yake, akamchukua yule mtoto mdogo, akaja mbele yao na kumweka katikati yao, na akamkumbatia akiwaambia "mtu akimpokea mtoto mmoja wa namna hii kwa jina Langu, anipokea Mimi, na akinipokea Mimi, humpokea Yeye Baba wa mbinguni aliyenituma."

Mtoto huyu alikuwa na bahati kupakatwa na Yesu maana Yesu anawapenda watoto. Watu wote wazima wakawa wanasikiliza, maana walitaka kujua ni nani mkubwa. Hoja ya ukubwa iliwasumbua sana wengi siku hizo, kama ilivyo siku hizi. Hakuna anayetaka kuwa mfanyakazi, yaya, dereva au shamba boi wa mtu mwingine. Kila mtu anataka awe bosi. Jambo la kufahamu ni kuwa nafasi zote za kazi katika maisha ni za muhimu. Nilipata kazi ya kusafisha choo kwa miaka mingi nikiwa chuoni. Na nilifikiria mara nyingi, kama shule, ofisi au kanisa lisipokuwa na msafisha choo, je mambo yangekuwaje? Je mtu asipopata mtu wa kumlelea watoto wake, yaani yaya, mambo yatakuwaje? Umeshawahi kufikiria kazi hizi ndogo ndogo tunazozikwepa zilivyo na umuhimu maishani? Mitume walikuwa wanawania sehemu ya uwaziri mkuu, waziri au makamu wa rais, pale Warumi watakapoondolewa.

Yesu akasema yeyote anayejishusha na kuwa na roho kama ya mtoto, basi huyo ufalme wa mbinguni ni wake. Akasema wachunge sana, mtu yoyote asimchukie au kumtendea uovu mtoto, kwa kumnyanyasa au kumwonea, kwa maana kila mtoto ana malaika, na malaika wao wanautazama uso wa BABA wa mbinguni kila wakati. Akawaambia si mpango au mapenzi ya Mungu mtoto yeyote apotee au asiende mbinguni. Akasema kama mzazi au mtu mzima yeyote anawafanya watoto wafanye dhambi, basi afadhali afungiwe jiwe shingoni na kutoswa baharini kuliko kuishi. Maneno haya ni mazito sana. Kweli Yesu anapenda watoto, na hakuna linalomtokea mtoto asilolijua, Yeye na malaika wa mbinguni. Endapo yeyote anamwonea mtoto, kwa njia yeyote ile, au kumweka majaribuni, akae chonjo maana atakuwa anamfanyia Yesu Mwenyewe ubaya ule. Waweza kuona jinsi watoto walivyofurahi waliposikia Maneno yale, wakawa tayari kumtii na kumfuata Yesu. Mama wengine wakaleta watoto wao msululu kwa msululu ili tu awabariki, na kuweka mikono Yake juu ya vichwa vyao. Napiga picha jinsi palivyokuwa na vicheko vya watoto mahali pale.

Yesu akataja majina yao na kuwawekea mikono akiwabariki na kuwakumbatia. Lazima Yesu aliwapa ushauri wazazi "waleeni katika njia iwapasavyo mkiwaelekeza kwa BABA yao wa mbinguni, wamtumaini na kumtii na kushika maagizo Yake." Wengine walipojaribu kusema mwalimu ana shughuli tele Yesu alichukua muda na kuwabariki watoto kwa kuzungumza nao. Utafiti unasema 75% ya watoto wanamwamini Mungu kama Mwokozi wao, kabla hawajafikia miaka 10, na asilimia 90% kabla hawajafikia miaka 15, ila ni asilimia 3 tu ndiyo wanamwamini Mungu baada ya miaka 51! Watoto ni wanafunzi kamili wa Yesu kama watu wazima. Wanazaliwa wapagani ila wakiwa wanamjua Yesu, na tukiwaeleza habari za Yesu, wanamchagua katika maisha yao. Hebu wazazi tuepuke tabia ya kufukuza watoto

kwa kuwatukana matusi makubwa makubwa. Watoto wana hisia, na akili, tusifikiri nao si watu kamili. Tujiulize kama maneno ya kuumiza tunayowaambia yangekuwa yametamkwa kwetu, Je, tungeyapenda?

Tambua kwamba watoto wetu hawa, wakati tutakapofika mbinguni watakuwa kaka zetu na dada zetu si watoto wetu. Mzazi chukua muda kuwabariki, na kusema maneno ya baraka kwao. Watoto wa Kiyahudi, waliwekewa mikono na wazazi wao vichwani na kubarikiwa kila mara. Maneno mazuri ya baraka kwa watoto yanaenda mbali. Siku moja utafurahi kwa kuwaambia maneno ya baraka uliyotoa kama mzazi; maana mzazi amepewa mamlaka ya kumbariki mtoto wake, au kumlaani kwa matendo yake. Mtoto naye anapaswa kusikiliza njia ya Mwenyezi Mungu na kuitii, pamoja na kumtii mzazi wake.

Kuna watu ambao ni dhaifu pia kanisani, kama watoto japo ni watu wazima. Hawa tuwe waangalifu nao kama tunavyokuwa waangalifu kwa watoto ili tusiwaumize. Je Yesu alikuwa na maana gani aliposema ufalme wa mbinguni ni wao? Je alikuwa ana maana kila mtoto ataenda mbinguni? La! Hasha! Kuna watoto wengine ni jeuri, wasiotiii, wenye maneno machafu, wanaongalia picha chafu, wanaoimba nyimbo za ovyo, na hawana usafi wa moyo. Wana mawazo, maneno na matendo maovu. Hawa wakienda mbinguni watafanya mbingu kuwa nyumba ya huzuni, wakiharibu hata vipande vya dhahabu na lulu kwenye mji ule kwa kuvikata vipande vipande.
Yesu alikuwa anazungumzia watoto ambao ni wasikivu, ambao mawazo yao hayajachafuliwa na ukorofi; wale ambao wakikosea wanaomba msamaha na wanataka kuweka mambo yawe sawa. Alikuwa anazungumzia watoto ambao wanataka kusaidia wazazi wao kazi na kutii, hawajifikirii wenyewe, bali wanajikana nafsi. Mbingu itakuwa na watu wa namna hiyo. Kama hatuna hii tabia sasa, Mungu anatupa muda tubadilike, ili tusiachwe. Anataka tuje Kwake Naye atatufanya wapole, watiifu, wavumilivu, na wenye kutunza amani. Kumbuka hata Yesu Naye alikuwa mtoto na mvulana mdogo kisha akakua, hivyo anajua maana ya kuwa mtoto na shida zake.

Baada ya hapo, Yohana akamwambia Yesu, walimwona mtu akitoa pepo kwa Jina Lake, wakamkataza maana hafuatani nao. Walikuwa wameona wana hati miliki ya Yesu. Kwamba ni wao tu na si wa watu wengine wenye kibali cha kutoa mapepo. Hapa walifanya kama Yoshua alipoona Eldadi na Medadi wanatabiri, akamwomba Musa awakataze hao. Basi Yesu akawaambia "msimkataze, kwa kuwa hakuna atakayefanya muujiza kwa ajili Yangu na kuweza kunisema vibaya, maana yule asiye kinyume Changu yu upande Wangu." Akasema yeyote atakayewapa kikombe cha maji kwa kuwa wao ni watu wa Kristo, hatakosa thawabu yake. Ila yeyote atakayemkosesha mtoto mdogo anayemwamini Mungu, ni afadhali afungiwe jiwe la kusagia shingoni mwake na kutupwa baharini. Hii ni adhabu kubwa, yaani kifo. Mtu yeyote anayefanya mwingine asiende mbinguni, bora afungiwe jiwe azame, yaani asitembee duniani tena.  Hakika hii ni Adhabu nzito.

Akasema mkono wa mtu ukimkosesha bora aukate, kwani ni afadhali kuingia mbinguni na mkono mmoja, (na hata hivyo utaota mwingine!), kuliko kwenda Jehanamu kwenye moto wa milele na kupoteza viungo vyote. Akasema mguu

ukimkosesha mtu, aukate maana ni afadhali kuingia mbinguni kiwete, kuliko kwenda Jehanamu na miguu miwili na kuungua moto. Jicho likikukosesha ling'oe, na litupe maana ni afadhali kuingia mbinguni chongo kuliko Jehanamu kwenye moto na macho mawili. Hata hivyo kila atakayekwenda mbinguni kilema atarudishiwa mwili wake kuwa mkamilifu tena. Chumvi ni njema ila chumvi ikiharibika haifai kwa lolote. Basi akawaambia wawe chumvi na kukaa na amani wao kwa wao kwa mapenzi au ladha nzuri. Yesu anajua yote, yale tunayokutana nayo, na tunapoishi, majumbani mwetu, na kila kitu.

*Omba kwa ujasiri mtakatifu kwa kumrudishia Maneno Yake- "Mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho nanyi mtapewa. "Unapoomba, wasilisha ahadi hii. Ni fursa ya upendeleo kwetu kumwendea Yeye tukiwa na ujasiri mtakatifu. Tukiwa dhati na wanyofu tunamwomba Aache nuru Yake iangaze juu yetu, Yeye Atatusikia na kutujibu.
--------------------------

Maswali: Mtu anawezaje kuwa kiongozi na pia mtumishi? Yesu alikuwa na maana gani aliposema 'kukata mguu, au mkono?" Je tufanye nini ili tumtazame Yesu na si uongozi ulio na uovu? Kwa nini mitume walimkataza mtu asitoe pepo? Yesu alikuwa na maana gani akisema kung'oa jicho?

**SIKU YA 249.**
**(Septemba 5)**

# Je, ni halali kumpa mke talaka au kuachana?

**Marko 10.**



Mafarisayo wakamwendea na kumwuliza ili wamweke mtegoni "Je ni halali mtu kumwacha mkewe?" Wakamjaribu. Siku zile ilikuwa mwanamume ndiye anampa talaka mkewe, bali siku hizi wanawake pia wanawapa talaka waume zao. Wengi waliacha wake zao, ili waoe wengine waliofikiri wanawafaa au walio vijana zaidi. Jambo hili lilimsikitisha BWANA, maana ndoa ni agano kati ya mume, mke na Mwenyezi Mungu. Naye Mungu alimwumba Adamu na Hawa, si Adamu, Hawa, Amina na Rehema. Mafararisayo walijali kushika sheria ya kwenye karatasi, na wala si upendo kwa wake zao.

Yesu akawauliza "Musa aliwaamuru nini?" Wakamwambia Musa aliruhusu kutoa hati ya talaka na kumwacha mke. Yesu akawaambia, Musa alifanya vile kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, ndiyo maana aliandika amri hii ya talaka. Ila toka Mungu aumbe ulimwengu, mwanamke na mwanamume, hawakuwahi kutenganishwa. "Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye naye ataambatana na mke wake, na hao wawili watakakuwa mwili mmoja, hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja, basi kile alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe." Hizi ni hesabu za ajabu za Mungu. Naye anasema na Baba Yake, na Roho Mtakatifu ni kitu kimoja.

Watu walishangaa, kwa kuwa walikuwa wamefikiri kuoa na kumwacha mtu ni kitu rahisi, wasijue kwamba ni Mungu huwaunganisha yule mke na mume, na ni mojawapo ya taasisi za kwanza kabisa Mungu alizoanzisha/alizoweka. Japo mume au mke walimchagua wao wenyewe, bado mume au mke ana jukumu kwa Mungu kumtunza huyo mke au mume, kumlinda na kukaa Naye milele. Ndiyo maana kwa Waswahili ndoa huitwa pingu ya maisha. Haipaswi kuwa pingu ya huzuni bali ya furaha, wala mwanandoa asitazame huko na kule kutafuta mwingine. Hata leo wengi wanaoachana wanarudi kuoa mtu mwingine, ambapo Yesu alisema kufanya vile ni kuzini. Mtu akiachana yapasa akae mwenyewe, asioe tena labda iwe kwa sababu ya uzinzi au kifo. Hata hivyo wengi hurudi kuoa kwa kuwa walitoka kwenye ndoa si kwa vile hawataki ndoa, bali walitaka kubadilisha mtu mwingine. Kufanya hivyo ni kuwa na mitara (serial polygamy/polyandry).

Nyakati za Malaki watu walitaka wake ambao ni vijana. Hawakupenda wake ambao ni wa rika lao, bali wale wadogo kwa umri au wa rika la watoto au wajukuu wao; wakafikiri kwamba wao hawazeeki daima. Jambo hili ni gumu, hasa kwa watu wa sasa ambao inakuwa vigumu kuishi na wengine, maana jamii haitegemeani kama zamani. Mume apaswa kumpenda mke wake wa ujana kama Kristo anavyolipenda kanisa, hata akafa kwa ajili yake, na mke apaswa kumtii mume wake, ndiyo maagizo ya ndoa kwenye Maandiko matakatifu. Mume ni kichwa cha mke wake, na mke ni msaidizi wa mume wake. Mwanamume ndiye aliyepewa kuwa mtawala, na mkewe kuwa msaidizi.

Msaidizi ni wadhifa mkubwa. Roho Mtakatifu ni msaidizi, ila haimaanishi kuwa ana hadhi pungufu. Kila mtu anataka kufanya anavyotaka, kuoa akitaka, au kuacha akitaka. Wengine wamesema hawahitaji kuoa ila wanaishi na mtu bila ndoa. Mungu aliyeanzisha ndoa alijua tunahitaji ndoa, ila uvumilivu unaonekana kuwa mdogo. Hii imeleta huzuni kwa mke, watoto na mume mwenyewe. Yamekuja mambo mengi siku hizi ambayo ni mbadala wa ndoa, na mengine yamehalalishwa na serikali, hii haijalishi, yapaswa turudi kwenye Maandiko Matakatifu, na kuona kama yamehalalishwa humo, pia. Kama, la! Yapaswa tuyaepuke mazoea au mahusiano hayo.

Mtu anayetaka kuoa awe mwangalifu maana kuachana si mpango wa Mungu. Ni muhimu kumwomba Mungu ili akutafutie mtu mcha Mungu mwenye matendo mema na mnayepatana katika tabia. Ushauri wa Maandiko matakatifu na wa watu wazima wanaompenda Mungu ni muhimu sana kwani wanaona kile vijana hawaoni wakiwa na 'upofu' wa mapenzi. Haya ni muhimu, maana kukutana na mtu wa kuoa kwenye baa, jumba la dansi, kwenye uchawi, au vificho vya giza, yaweza kuwa huzuni kubwa kwa wale wanaompenda Mungu.

Mtu mmoja ameandika hivi "Ikiwa kuna somo lolote ambalo linapaswa kuzingatiwa kwa utulivu na uamuzi usio na mihemko yenye misukumo, ni somo hili la ndoa. Iwapo Biblia inahitajika kama mshauri, basi ni kabla ya kuchukua hatua inayowaunganisha watu wawili, yaani mke na mume maishani. Lakini hisia iliyopo ni kwamba katika jambo hili hisia za mahaba makali ndio ziwe mwongozo; na katika hali nyingi sana hisia za mahaba feki au ugonjwa wa mapenzi (infatuation/lovesick) huchukua

usukani, na kuelekeza kwenye uharibifu fulani. Ni hapa ambapo vijana huonyesha akili ndogo kuliko somo jingine lolote; ni hapa kwamba wanakataa kushauriwa na kujadiliana na wale wenye hekima. Suala la ndoa linaonekana kuwa na nguvu za kuwaroga. Hawajisalimishi kwa Mungu. Hisia zao zimefungwa minyonyoro, nao wanasonga mbele siri, kana kwamba wanaogopa kwamba mipango yao itaingiliwa na mtu fulani." FE 103.1. Mahusiano ya uchumba kabla ya kufanyika inabidi hisia kali za mapenzi ambazo ni za kipumbavu au zisizo na busara, zilizopitiliza kimihemko na zinazomfanya mtu kufanya mambo kwa siri akiamini ikijulikana kuna mtu atavuruga, ziondolewe mawazoni mwetu kwa msaada wa Mungu. Kwa kifupi tafuta wenye busara wanaompenda Mungu, walio watu wazima kukushauri. Maisha ni kuvumiliana. Kila mtu ana kitu anachokivumilia kwa mwenzake. Hata wale wanaoishi na wazazi, kaka na dada wanavumiliana. Tunajuaje hili basi? Magazeti yanazungumzia magomvi na mauaji katika mahusiano yote, iwe ni binamu, shangazi, wazazi, babu au wanandugu. Kwenye ndoa kwa vile watu huishi pamoja kwa miaka mingi kuliko muda wanaoishi na wazazi wao, huchangia mambo yote pamoja kuliko na wazazi, na kwa hivyo watu hutoana dosari zaidi kuliko kwenye mahusano mengine. Ipo haja ya kutilia maanani kwamba ndoa ni taasisi na mpango wa Mungu na Shetani akiharibu ndoa anajua ameharibu familia, jamii na taifa. Mataifa yaliyotawala dunia, kama vile Ugiriki, kwenye Danieli 2, yalianguka kutokana na matatizo ya kifamilia. Kutokana na ukweli huo Shetani amekuwa akiipiga vita ndoa usiku na mchana. Hebu tuwe macho kama vijana na watoto wa Mungu tufanye sehemu yetu pia.

Yesu alipofika kwa wanafunzi Wake, hao wakamwuliza kuhusu lile alilosema. Naye akawaambia; Kila mtu anayemwacha mkewe na kuoa mwingine amefanya dhambi ya zinaa, na mke akimwacha mumewe na kuolewa na mwingine naye pia anavunja amri ya saba kwa kuzini. Twahitaji uwezo toka kwa Mungu ili kuishi katika familia, kisha tuombee ndoa za wazazi wetu, nasi tusiwe sababu ya kuleta matatizo kwenye ndoa hiyo. Hatupaswi kujadili shida za watu katika ndoa, ila, wale watu wazima ni jukumu lao kuwasaidia walioanguka katika jambo hili, kwa upendo, na kwa kadri wanavyoweza.

Wanafunzi wakasema mambo ya mtu na mkewe yakiwa hivyo, basi haifai kuoa; bora kukaa mseja. Yesu akasema si wote wawezao kulipokea neno hili la kutooa maana kuna watu ambao ni matowashi, hawa hawakuoa. Waweza kuwa walizaliwa vile kwa upungufu fulani wa mwili na hivyo hawawezi kuoa au kuolewa. Na wengine wamekuwa matowashi kwa kudhamiria wenyewe ili wapate kufanya kazi ya Mungu bila kushugulikia mahitaji ya familia. Na kuna wengine wamefanywa kuwa matowashi na wenzao kama wale vijana wa Babeli waliomtumikia mfalme walikuwa wamefanywa kuwa matowashi, na mfalme ili washughulike katika mambo ya ufalme na si ya familia. Akaongeza "Awezaye kulipokea Neno hili na alipokee." Tuelewe kwamba mtu anayesema kwamba haoi wala kuolewa si yule anayekaa na mwanamwali au mwanamume bila kupata cheti cha ndoa, akisema sijaoa au kuolewa wakati anakaa na mtu kama mume au mke wake. Huyo asijidanganye ni mzinifu na mwaasherati. Anafanya jambo lisilopendeza mbele za Mungu. Ila serikali zetu huwa zinahesabu ni ndoa watu wakikaa pamoja kwa miaka 2, ili mtu asipoteze mali au haki walizochuma pamoja au watoto wanaopata wakiwa katika mahusiano

hayo ambayo hawakupanga kuyahalalisha waweze kupata matunzo.

Umeshawahi kuishi na watu wanaokuja kila mara karibu nawe ili kukutega, kukukosoa, na kufanya maisha yako yawe ya huzuni, na kuonekana kama hawana kazi nyingine maishani mwao kwasababu shetani anawasumbua? Hayo ndiyo yalikuwa maisha ya Yesu, hakukuwa na vyombo vya habari, au televisheni au simu au radio, ila walisafiri mbali na kila mahali kumfuata Yesu, ili kutafuta lawama, mashitaka, na uovu wa namna fulani. Ila hawakufanikiwa hata siku moja kumwona akitenda dhambi. Kwasababu maisha Yake yalikuwa makamilifu, kila walipomtafutia uovu mahali ili wamshike hawaweza. Mwishowe walisema “Amesema Yeye ni Mungu”. Sasa hapo hakukuwa na cha kupinga, kwani Yeye Mungu!

*Mbingu iko wazi kwa ajili ya maombi yetu, na tunaalikwa kwenda “kwa ujasiri kwenye Kiti cha Neema, ili tupate rehema, na kupata neema ya kusaidia wakati wa shida.” Tunapaswa kwenda kwa imani, tukiamini kwamba tutapata vile vitu tunavyoomba Kwake.

-----------------------------

Maswali: Je Kwa nini Mungu hapendi mtu na mke wake waachane? Je ni shida gani mke, mume na watoto zinawapata talaka ikitolewa? Kwa nini binadamu wasitenganishe kile ambacho Mungu amekiunganisha? Ni watu gani wanaweza kukaa bila kuoa au kuolewa? Kwa nini ndoa ni taasisi muhimu sana?

**SIKU YA 250.**
**(Septemba 6)**

# Waacheni watoto wadogo waje Kwangu.

**Mathayo 13, Marko 10**



Wazazi na hasa akina mama wakamletea Yesu watoto wao, awawekee mikono juu ya vichwa vyao ili awabariki na kuwaombea. Wazazi hawa walikuwa na uhakika Yesu ataleta tofauti kwenye maisha ya watoto wao; wakapenda awabariki ili kuyafanya maisha yao yawe na thamani na baraka kwao na jamii yote. Hata leo wazazi wengi wanapenda mema kwa ajili ya watoto wao, wanaleta watoto wao kwenye nyumba za ibada au kwa viongozi wa Kiroho ili wabarikiwe. Wanafunzi, kama watu wazima wengine waliona BWANA wao ana shughuli nyingi na amezingirwa na watu wengi, na sasa wazazi wanamchosha na vitoto vidogo, wakawakemea hawa wazazi.

Lakini Yesu alichukizwa sana na jambo hili akasema "waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao. Amini nawaambia Yeyote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa." Akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, akawabarikia. Je usingependa kuwa moja wapo wa watoto hao waliobarikiwa na BWANA

Mwenyewe? Napenda kufikiri kwamba watoto hawa walikuwa watoto bora kupita wote vijijini mwao. Maisha yao yalikuwa na mvuto wa mambo mema, ya kusaidia watu, kuongoza watu kumpenda Mungu, na huduma zingine mbali mbali.

Wakati injili inahubiriwa duniani kote kukaribisha ujio wa Yesu, watoto wengi wanashiriki katika shughuli hii. Kule Brazil mtoto mdogo Victoria aliye na umri wa miaka tisa, tulimwona akitumia makasia na mtumbwi mdogo kwenda kwa wenzake kijiji cha jirani kusoma nao Biblia. Watoto wanaamini kirahisi, na wanakuwa na wanamtumainia Mungu, hawana muda wa kufikiria mabaya kwanza kwa sababu madoa yao ya uovu ni machache.

Katika mila na destruri za siku zile, watoto wa Kiyahudi walikuwa na bahati kubwa kwani mataifa mengine kama Waamoni walitoa watoto wao makafara, wakifikiri itafurahisha miungu yao kwa kuondoa balaa au kuwapa mali na cheo. Watoto wengi mahali pengi wamenyanyaswa kufanya kazi mashambani kwa masaa mengi, kuliko watu wazima na haki zao za kibinadamu zimepotea. Kawaida mzazi anampenda mtoto kuliko mtoto anavyompenda mzazi, na ni vigumu kuamini kwamba kuna watu wazima ambao wanawafanyia watoto ukatili na uovu wa hali ya juu, kama huu au mwingine unaoendelea.

Watoto wengi hufanyiwa ukatili na wale watu ambao wako karibu nao. Twapasa kuwalinda watoto wetu, na wa jumuiya tunayoishi kama watu ambao tunampenda Mungu. Mamilioni ya watoto wananyanyaswa kwa kupigwa, kubakwa, kutengwa, na kuachwa bila msaada, iwe ni majumbani mwao, vituo vya watoto yatima, mashuleni au kwenye jumuiya. Takwimu nyingi hazipo wazi maana vitendo hivi vinatendwa kwa siri. Unyanyasaji ni matumizi ya makusudi ya nguvu kimwili yenye kutishia kuwaletea watoto madhara ya kisaikologia, kifo, na kuwanyonya kibiashara, kingono, utesaji wa kimwili au haki zao kama binadamu.

Watoto wengi wametelekezwa, hawajaliwi na hawasaidiwi na familia au jumuiya kimaendeleo. Hawa hawaendi sambamba na urithi au mazingira yao. Haya yamesababisha watoto wawe na magonjwa yasiyotibika, kudumaa, na mengine ya kuhuzunisha. Wanyanyasaji wengi ni wazazi, walezi, walimu, waajiri, na wanafunzi wenzao. Asilimia 20-65 ya watoto wametendewa vibaya mashuleni na wenzao, au walimu bila kupata msaada. Takwimu ya miaka 10 iliyopita yasema watoto wa kike 150 milioni na wa kiume 73 milioni walibakwa duniani. Wengi wanajiuliza kwa nini jamii na familia zinatelekeza watoto kiasi hiki? Mungu ana huzuni kwa hili, nasi kama watu tunaompenda Mungu hebu tuwe watetezi wa hawa watoto, maana kuna siku ya hukumu, na huko tutatoa hesabu.

Mtoto akifika miaka mitatu hivi tabia yake imejengeka, na saba tabia yake imekamilika, hivyo yale tunayofanya kabla ya miaka saba ni muhimu. Mtu mmoja aliandika kitabu akisema "yote ya muhimu niliyopaswa kuyajua kama binadamu nilijifunza kabla ya kumaliza chekechea. Mtoto anajifunza mengi miaka saba ya mwanzo ya maisha yake. Wazazi wachukue muda kuweka malengo, na upendo katika miaka hii. Chakula anachokula mtoto kiwe rahisi na si vyakula vya kuigiza kwenye runinga au mahali fulani. Vyakula vilivyokobolewa na kusindikwa ni vibaya

sana kwa mwili unaokua na hata wa mtu mzima. Vyakula hivi vinaathiri tabia ya mtoto. Hebu kila familia iwe na bustani, maana tabia ya mtoto inakuwa bora akiwa na kilimo kwenye ratiba yake, kwani atajua kula chakula bora na anayependa kazi. Kilimo ndiyo ABC au Alfabeti ya Elimu. Mtoto asiwe mvivu apotezaye muda kwa kukaa bure na kushugulikia maovu.

Chakula ni muhimu pia kwa tabia ya mtoto kushinda majaribu na kujikana nafsi. Haya waliambiwa wazazi wa Samsoni, Yohana mbatizaji, Yesu na wengine. Mtoto asipewe chakula cha aina fulani mfano chenye mafuta mengi, sukari nyingi, chumvi nyingi au kilichokobolewa. Mtoto asiwe anakula ovyo ovyo siku nzima. Apangiwe milo ya kula baada ya masaa mane au matano. Hata mtoto anayenyonya akae masaa matatu hivi kabla ya mlo mwingine. Huyu anaweza kujengewa ratiba kwa wiki chache na akafuata. Kula kula ovyo, kunaleta shida ya kutawala tabia na kujilinda na majaribu. Chakula, hasa kibaya, kama chenye masukari mengi kinaleta aina ya ulevi au uraibu, na mtu akianza kukipenda ni vigumu kukiacha. Tukumbuke Hawa alituleta katika dhambi, kifo na maumivu tuliyo nayo kutokana na chakula. Naye Esau aliuza urithi wake kwa chakula.

Wakati wa wafalme wabaya kama Manase, watoto walitolewa kafara, na kuwa kitu cha Huzuni kwa Mungu wa mbinguni. Watoto wapaswa waelimishwe vizuri kwa Maandiko Matakatifu na kupewa weledi au urithi wa elimu, mtaji au ardhi ili waweze kujitegemea. Jambo zuri kupita yote mzazi atakalomfundisha mtoto wake ni 'kumwezesha aishi bila yeye'. Mzazi asizae bila malengo ya kumsaidia mtoto ajitegemee, au kuwa na magoli kwa mtoto. Masomo muhimu mtoto yeyote anayopaswa kujifunza ni utii kwa Mungu na kwa binadamu, kujikana nafsi, kupenda kazi, mpangilio wa mambo, kuhudumia wengine, nidhamu, uaminifu, na usafi wa mwili na moyo. Muda na upendo ndiyo zawadi kubwa mzazi atakayotoa kwa mtoto, na si vitu. Sote kama wazazi lazima tuwe na mkakati wa kujifunza mara kwa mara jinsi ya kulea, na kufanyia kazi tunayojifunza. Siku hizi masomo ya Jando na Unyago yamepotea, ambapo mengine yalikuwa msaada, hivyo ni vyema wazazi wakutane na kujifunza na kufunza watoto wao. Watoto wana maswali mengi na udadisi, wasipopata mafundisho mema, watapata mbadala kwa mwingine ambaye si sahihi, na aweza kuwa adui wa Mungu.

Wazazi wasijifikirie wenyewe na shughuli zao. Tunaelewa fika kila mzazi ana mizigo yake katika malezi. Hata hivyo, vile tuishivyo, ni muhimu zaidi kwa kuwa watoto hawazingatii sana yale tunayosema, bali zaidi sana yale tunayoyatenda hivyo mitindo yetu ya maisha iwe na maadili bora kwa neema za Mungu wetu Mwenye upendo. Ikiwa baba anataka watoto wake waende kwenye ibada, ila yeye mwenyewe haendi ni lazima atavuna uovu huo anaopanda. Muda ambao baba anautumia na mtoto wake nchini Marekani kwa siku ni pungufu ya dakika saba. Kina baba wana sehemu kubwa katika malezi ya watoto, hivyo wasilitelekeze jukumu hili muhimu. Biblia inazungumza jukumu la baba na mama katika kutunza mtoto. Siku ya hukumu wakina baba na wakina mama wataulizwa "liko wapi kundi lako dogo nililokupa?" Tukisoma maisha ya Ibrahimu, twaona alisifiwa na Mwenyezi Mungu, kwamba "anajua kusimamia nyumba yake." Je na sisi Kwa nini tusiombee wazazi wetu, ili Mungu awasaidie kusimamia nyumba zetu kwa mpango wa Mungu? Zawadi ya

pili kubwa ambayo baba atampa mtoto wake, ni kumpenda mama yake, na mama naye, zawadi kubwa atakayompa mtoto wake ni kumtii n a kumpenda baba yake yule mtoto. Hii ni pamoja na kusema maneno mazuri na kutogombana mbele ya watoto au kutumia maneno ya kutisha. Wengi wamesikika wakitamka maneno bila kumaanisha kwa ajili tu ya hasira. Utasikia mtu akisema, "mbwa wee" na mengineyo mengi. Kwa kweli ni makosa kumlinganisha binadamu na mbwa, kwani binadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Wazazi wanapaswa kuwa na maneno ya kutia moyo, nayo yatampa mtoto ujasiri kukazana na kukomaa katika maadili na stadi muhimu vyema.

Tuchunge midomo yetu, maana maneno yote tuyasemayo, yataletwa hukumuni; yawe yale tunayomaanisha au yale tusiyomaanisha, yote yataletwa. Tumwombe Mwenyezi Mungu atupe nguvu na uwezo wa kutii. Wazazi pia wamesikitishwa na watoto wao waliokuwa wakaidi, wasiotii, au wanaotaka kutawala wazazi na familia yote; hatimaye wakaingia kwenye mashimo ya ulevi, ujambazi, umalaya, uchafu wa tabia, au uovu wa kila namna na hata kuhuzunisha wazazi kwa hali ya juu.

Watoto pia kwa upande wao wamefanya vibaya kwa kuwatelekeza wazazi waliowakuza kwa upendo mkubwa. Huu nao ni uovu mkuu. Ni jukumu la mtoto kutunza wazazi wake wakiwa wazee kwa hali na mali. Hii ni amri ya tano, na ya pekee yenye ahadi. Wazazi wasikate tamaa bali wawaombee watoto wao kama 'baba wa mwana mpotevu', alivyofanya. Waombe hekima jinsi ya kuchukuliana nao, maana watoto ni watu kamili na wana uchaguzi wa jinsi wanavyotaka kuendesha maisha yao. Tumeambiwa tuwapende watoto wetu, na hasa wakati tunapokuwa katika kuwarudi au katika kuwaadhibu. Uchapaji wa viboko wakiwa wadogo, uzingatie kanuni hii ya upendo. Tuhakikishe kuwa upendo wetu unazidi adhabu au vile viboko tunavyotoa. Mtoto ajue kosa lake kwanza, na kuna haja ya kumwomba Mungu unapotoa adhabu ili iwe msaada kwa pande mbili.

Kamwe, tusipige au kuadhibu watoto kwa hasira. Upendo wetu, mara zote uzidi adhabu na ghadhabu zetu. Wengi wamepiga watoto na kuumiza na hata kuua. Hili linamhuzunisha Muumba wao. Kama upendo wetu ni mdogo, na adhabu zetu ni kubwa, hiyo inadhihirisha kuwa hatuna haki ya kutoa adhabu hizo, na badala yake inatupasa kuzisitisha. Yesu alisema maneno makali kwa watu wazima, kwamba wakiwakosesha watoto wadogo kuingia katika uovu, basi imewapasa wafungiwe jiwe shingoni na kutupwa kwenye maji, ili wazame chini na kufa; washindwe kuogelea au kujiokoa. Hebu ukali wa kupita kiasi na ukatili wetu wazazi usifanye watoto kufikiri mbinguni ni mahali pabaya na kisha wasijitahidi kuwepo huko. Hebu wazazi na watoto watilie maanani maneno haya kwani wote ni warithi wa ahadi na neema za Mungu kama wao. Tuombeane, maana hata nasi tuna changamoto, ila Mungu atatushindia, kwa Jina Lake tukufu, amina!

*Kila ahadi katika Neno la MUNGU huja pamoja na mada ya kuombea, ikileta Neno la Yehova lililoahidiwa kama uthibitisho kwetu. Baraka yoyote ya kiroho tunayohitaji, tumependelewa kuiomba kupitia Yesu. Tunaweza kumwambia Bwana, tukiwa na unyenyekevu wa mtoto, kile tunachohitaji haswa. Tunaweza kumwambia mambo yetu ya muda, tukimwomba mkate, mavazi na Mkate wa Uzima na vazi la

haki ya Kristo. Baba yako wa mbinguni anajua kuwa unahitaji vitu hivi vyote, na umealikwa kumuomba juu ya vyote. Ni kwa kupitia  Jina la Yesu ndiyo kila neema (feva) inapokelewa. MUNGU ataheshimu Jina hilo, na atakidhi mahitaji yako kutoka katika utajiri wa ukarimu Wake.


----------------------------

Maswali: Yesu alifanya jambo gani lililoonyesha thamani ya watoto? Je mambo gani siku hizi watu wanafanya yanayoonyesha watu wazima hawathamini watoto? Kwa nini ni muhimu kuwapeleka watoto kanisani ili wabarikiwe? Kwa nini ni muhimu kutoa sadaka kwa Mungu mtoto anapozaliwa, kama vile ilivyo umuhimu kufanya sherehe ya kuzaliwa? Kwa jinsi gani twaweza kusema wachanga katika imani ni watoto pia?

**SIKU YA 251.**
**(Septemba 7)**

# Kijana tajiri na mtawala.

**Marko 10. Mathayo 13.**



Yesu alikuwa anatoka kwenda njiani, akamwona mtu anapiga mbio kwa vishindo akija Kwake kumfuata kisha akapiga magoti. Huyu alikuwa kijana, tajiri, na kiongozi. Huyu alikuwa tofauti na viongozi wengine waliokuwa wapelelezi wanaotaka kumweka Yesu mtegoni. Umati wa watu wakashangaa amekuja na ujumbe gani mzito mtu huyu, aliyevalia mavazi ya gharama na mazuri hivi? Huku akiwa bado anahema, akamwuliza Yesu "Mwalimu mwema nifanye nini nipate kurithi uzima wa milele?" Huyu kijana aliona matendo yake tu ndiyo yatamwezesha kuingia mbinguni. Yesu akamwuliza, kwa nini kuniita mwema, ni mmoja tu aliye mwema, Naye ni Mungu. Akamwuliza kama anazijua amri zinazofafanua mahusiano kati yake na binadamu wenzake yaani ile ya 5 mpaka ya 10 inayosema, "usiue, usizini, usiibe, usishuhudie uongo, usidanganye, waheshimu baba na mama yako, na mpende jirani yako kama nafsi yako."

Kumbe amri ni za muhimu!, vinginevyo mtu huyu asingeulizwa. Ila kutunza amri ni mwanzo tu wa safari. Yesu alileta kwake amri zile zinazohusu ujirani au watu akijua kwamba ndizo zilikuwa na hitilafu kwake. Mtu huyu akasema, mwalimu nimeshika haya yote toka ujana wangu; Yesu "akamkamkazia macho huyu kijana

na akampenda" kwani aliona ana mengi mazuri, na akataka awe mwanafunzi Wake. Alimpenda kwa vile alikuja kufa kwa ajili yake, akaona akijitoa kabisa asilimia 100, atafanya makubwa kwa kuwaambia watu wengine kuhusu Yeye, na kuhudumia au kusaidia watu wengine. Akamwambia ukitaka uwe mkamilifu "Umepungukiwa na neno moja, enenda ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate."

Maskini kijana huyu mwenye nguvu, mwenye nguo safi za gharama, aliyepiga magoti akiuliza kwa adabu, akitaka kujua cha kweli cha kufanya kwa maisha yake ya mbeleni, hasa aliposikia mafundisho ya Yesu siku za nyuma, alikuwa na mengi yanayoendelea moyoni mwake. Jambo lililopunguka lilikuwa KUBWA! Mali ilikuwa Mungu wake; alizipenda zawadi alizopewa na Mungu, bali hakumpenda Mpaji. Kumtii Mungu ni zaidi ya kuwa na adabu njema, ni kuishi kama Yesu alivyoishi, maisha ya kujinyima yaani kujikana nafsi. Aliondoka kwa huzuni pengine akifikiri "mimi nakuuliza jinsi ya kuingia mbinguni wewe unagusa mali yangu, sijakuuliza kuhusu vitu vyangu."

Yesu ni tabibu wa kweli anayejua ugonjwa wa kila mmoja wetu, na vidonge vya kumpa mtu huyo. Kijana tajiri, ugonjwa wake ulikuwa ni kuwa mshiriki au muumini bila kujitoa kikamilifu. Alipenda mali kuliko Mungu. Leo sisi pia tuna ugonjwa huo; tumwombe Mungu atuonyeshe ugonjwa wetu, na vidonge vya kuchukua, maana anajua mioyo yetu, nia zetu na mawazo yetu kuliko sisi tunavyojijua. Kila mtu ana ugonjwa tofauti na dozi tofauti! Mungu hajatutaka tuuze vyote, lakini je kama angetuuliza kufanya hivyo leo, tungekuwa tayari kutoa? Ni wale tu ambao wako tayari kutoa vyote; yaani hali na mali ndiyo watoto wa kweli wa Mungu. Kung'ang'ania vitu, yaonyesha moyo wetu upo kwenye vile vitu. Mtu amesema nieleze unavyotumia pesa zako, muda wako na wakati wako wa burudani, nami nitakwambia moyo wako uko wapi!

Njia pekee ya Mungu kutuokoa sisi binadamu ni kukata na kutupa vile vyote ambavyo vinaleta udhaifu kwenye tabia zetu na kutupeleka mbali na Mungu. Tunaporudisha vile ambavyo Mungu ametupatia, tunajiwekea hazina mbinguni. Furaha ya kuona watu wameokolewa na wako katika ufalme wa Mungu, ni zawadi ya pekee kutoka kwa Yesu, kwani tunafuata nyayo Zake, maana alisema "nifuateni." Mungu hatakupunja au kukudhulumu ukitoa, maana Yeye si dhalimu, anajua mahitaji yako, wewe mtegemee kikamilifu. Hakuna mtu aliyetoa kwa kazi ya BWANA au kusaidia wenye mahitaji akawa maskini. Hata mitume mahitaji yao yote yalikidhiwa maisha yao yote. Hata kama ana chenji yetu atatarudishia! Anarudisha kwa njia mbali mbali, yaweza kuwa mali, au afya, au furaha n.k.

Kijana huyu tajiri alidhania atakuwa maskini kama hawa Wagalilaya ambao wamekuwa wakitembea bila makao, na kuingia kwenye nyumba za watu ili walishwe, na hivyo kupoteza dira na njozi za maisha. Alifikiri, Je, nitaishi maisha ya namna hii mpaka niwe mzee? Palikuwa na ukimya, Yesu na wanafunzi wakimtazama. Basi naye kwa taratibu, akanyanyua miguu yake na kuanza kutoweka. Neno la Mungu lasema, "walakini yeye akakunja uso kwa neno hilo, akaenda zake kwa huzuni kwa sababu alikuwa na mali nyingi." Kijana huyu alikumbuka mashamba yake, magari

ya farasi, dhahabu zake, nyumba za fahari, watumishi na mifugo. Je yote haya anapaswa kuyatoa? Pengine Yesu alimwambia akauze vyote kwanza ndipo awape masikini, na si kuwapa maskini vitu vyake, ili asibadilishe mawazo na kwenda kuvichukua vile vitu tena kwa watu aliowapa. Hakika kama Masihi Mwenyewe alisema ni tajiri, basi alisheheni mali!

Kijana huyu alishindwa mtihani. Kijana huyu alijua anapungukiwa na kitu. Watoto wengi wanasoma, ili wapate kazi nzuri na hili ni jambo jema, maana hatuwezi kuishi bila pesa. Pesa yenyewe si mbaya ila kuipenda na kuitafuta kwa njia mbaya na kisha kuitumia kwa njia mbaya ndipo ulipo ubaya wa fedha. Ni kosa kubwa kuitegemea pesa, maana watu wengi wamejichoma kwa maumivu mengi kwa kuipenda pesa. Wanafunzi walifikiria kama mtu huyu tajiri anayeshika amri hawezi kuingia mbinguni Je, ni nani ataingia? Mtu huyu alipoteza nafasi ya kuwa mtume. Jina lake lingelitajwa kwa miaka maelfu, na kuandikwa kwenye misingi ya mji wa Yerusalemu. Alikataa nafasi ya kumfuata Mfalme wa wafalme, akitaka kushughulikia mali.
Hata leo sisi yawezekana tusiwe na mali ila tuna vitu tunavyovipenda moyoni, na hatuko tayari kuviacha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Safari ya mbinguni ni endelevu, kama tukiacha vitu, tutaulizwa je wivu tumeacha? Basi lazima kuwe na ukarabati tunaopasa kuufuata kutokana na tabia zetu. Yaweza kuwa ni michezo, chakula fulani, ndugu zetu na mambo mengine yanayoitwa miungu. Kijana yule ambaye hatujui jina lake, angekuwa mtume maarufu ambaye jina lake lingesikika mpaka leo. Nasi leo, kabla hatujamlaumu huyu kijana na kumshangaa, tujiulize au tumwulize Mungu, ni kitu gani kinachopungua katika maisha yetu! Nasi pia twende tukakishugulikie hicho kitu. Je ni uchoyo, Je ni kutokuwa na huruma, au upole, Je ni kutosamehe waliotukosea? Je ni kuwa waonevu au wakatili kwa watoto wenzetu (bullies), na kuwapiga? Je ni kuharibu vitu vya wazazi au kutowatii? Je ni udokozi au wizi, Je! ni mahusiano ya mahaba yasiyofaa au yenye uovu?

Tukisikia maagizo ya Mungu anatupa amri tutekeleze. Na kama tutaona ni ngumu hatuwezi, tupige magoti na kumwomba Mungu atujaze kile tunachopungukiwa, ili tuwe wakamilifu. Tumwombe tusitoke kamwe nje ya uso Wake kwa huzuni kama kijana tajiri, kwamba hatutaki kutii yale anayotuelekeza kwa faida yetu; maana mbinguni kuna mabilioni ya vitu ukilinganisha na vifurushi vichache au takataka alizokuwa nazo huyu kijana tajiri. Yesu akawaambia wanafunzi kwamba itakuwa shida kwa tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni. Ili kuweka msisitizo juu ya kauli yake alisema, itakuwa rahisi zaidi kwa ngamia kupenya kwenye tundu la sindano kuliko tajiri kuingia mbinguni. Wanafunzi wakisikia hili walishangaa mno, na kusema “Ni nani basi awezaye kuokoka?” Hawa walifikiri mtu huwa tajiri kwa vile anafuata amri za Mungu.

Ndipo Yesu akawakazia macho na kuwaambia “kwa wanadamu hilo haliwezekani, bali kwa Mungu yote yawezekana.” Nao wakamwuliza kwamba watapata nini maana waliacha vyote wakimfuata Yeye na hata Yesu alipopaa mbinguni waliendelea kufanya kazi Yake. Wengine waliuwawa kwa kumshuhudia Mwenyezi Mungu na wengine walikufa kazini mwa BWANA. Yesu aliwajibu kwamba wote waliomfuata hapa duniani, katika ulimwengu mpya atakapoketi Mwana-Adamu katika utufuku Wake, nao wataketi katika viti 12 wakihukumu kabila kumi na mbili za Israeli. Na

kila aliyeacha nyumba, ndugu, dada, baba, mama, watoto au mashamba kwa ajili ya Jina la Yesu, atapokea mara mia, na kuurithi uzima wa milele. Ila walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, maana akakayevumilia hadi mwisho ndiye atakayeokoka. Si kitu kuwa wa kwanza halafu ukaishia njiani. Kazi si kuanza tu, bali pia kumaliza vizuri.

Kumbuka goli la maisha ni kuwa na Yesu mbinguni milele. Hebu hilo goli uliweke kwenye kumbukumbu yako ya kila siku. Maana maisha yana makelele mengi na yanapiga upesi sana, na mambo ya muhimu yanazama kwenye zile kelele na hutayasikia kirahisi mpaka uwe na utulivu mkubwa.

*Tembea daima katika nuru ya MUNGU. Tafakari mchana na usiku juu ya tabia Yake. Ndipo utaona uzuri Wake na kufurahi kwa wema Wake. Moyo wako utaangaziwa na hisia ya upendo Wake. Utainuliwa kana kwamba umebebwa na mikono ya milele. Ukiwa na nguvu na nuru ambayo MUNGU hutoa, unaweza kuelewa zaidi na kutimiza mengi zaidi ya ulivyoona kuwa inawezekana hapo awali.
--------------------------

Maswali: Kwa nini kijana tajiri alimkimbilia Yesu? Je kwa nini tamaa ya mali ni hatari? Yawezekanaje mtu mwema kama huyu aliyeshika amri 10 asifike mbinguni? Je tajiri awezaje kuokoka? Kwa nini safari ya mbinguni yahitaji kujitoa au kujisalimisha kikamilifu 100%.

**SIKU YA 252.**
**(Septemba 8)**

# Waajiriwa asubuhi na wale wa jioni, walipwa sawa sawa.

**Mathayo 20.**

Yesu aliendelea kufundisha kwa mifano, kwani iliwafanya watu wawe makini kusikiliza. Watu walipenda masimulizi Yake mazuri, wakawa wadadisi kujua maana yake, na hili likawaongoza kujua ile Kweli wenyewe. Aliposema wa kwanza watakuwa wa mwisho, ndipo aliposema ufalme wa mbinguni umefanana na mtu mwenye nyumba aliyetoka alfajiri kwenda kuajiri wakulima awapeleke katika shamba lake la mizabibu wavune kwa wakati, ili matunda yasioze. Naye alipatana na vibarua wale kuwapa mshahara wa dinari moja. Akawapeleka kwenye shamba lake kuanza kazi, na akaona vibarua wengine saa tatu, wamesimama sokoni bila kazi, akawauliza mbona mnasimama bila kazi? Wakamwambia wanataka kazi, akawachukua waende kwenye shamba lake la mizabibu, na kupatana nao mshahara wa dinari.

Saa sita akaenda akapata wengine na saa tisa, na saa kumi. Na hata saa kumi na moja akaona watu wamesimama mchana kutwa bila kazi akasema Kwa nini mnasimama hapa? Wakajibu hakuna aliyetuajiri, basi akawachukua waende kwenye shamba lake la mizabibu kuvuna, wala hawakuuliza mshahara wakijua saa zimeenda, watakachopata ndiyo hicho hicho kitakuwa riziki yao ya siku hiyo. Kulipokuchwa yule mwenye shamba alimwambia msimamizi awaite wale vibarua ili awalipe ujira wao kuanzia yule wa alfajiri mpaka huyu wa saa 11 jioni. Akawapa kila mtu dinari moja, wa alfajiri na wa jioni. Wale waliokuja alfajiri walifikiri watapokea zaidi, maana walikuja mapema, wakaanza kunung'unika walipoona mishahara yao ni sawa wakasema "hao wa mwisho wametenda kazi saa moja tu, nawe umelinganisha mshahara wao na wetu, ambao tumestahili taabu na hari za mchana kutwa."

Yule mwenye shamba akasema "rafiki sikukudhulumu, hatukupatana dinari moja, chukua iliyo yako uende zako, napenda kumpa huyu wa mwisho sawa na wewe. Si halali yangu kutumia mali yangu nipendavyo? Jicho lako limekuwa na wivu kwa sababu ya wema wangu kwa wote? Vivyo hivyo wa mwisho watakuwa kwanza na wa kwanza watakuwa wa mwisho. Yesu alitaka wanafunzi wajue kwamba zawadi ya ufalme wa mbinguni inatokana na neema, na si kwamba ni ujira unaotokana na kuufanyia kazi. Kusamehewa makosa yetu na wokovu, ni zawadi kubwa toka kwa Mungu, na wala hatuna haja ya kukasirika kwamba Mungu amewasamehe wengine pia, maana zawadi hiyo ni Yake, Naye anaitoa anavyoona vyema. Tukiokolewa na kuingia katika ufalme wa mbinguni, hatupaswi kukasirika na kuhoji kwa nini wengine wameingizwa pia, kwani tumefadhiliwa nasi pia, na tumefanya dhambi nyingi pia katika maisha yetu.

Tukumbuke yule aliyekaa na Yesu toka alfajiri aliburudika kuwa na BWANA aliyempenda na kuzungumza Naye siku nzima, ukilinganisha na aliyekuja mwisho, ambaye pengine alibondwabondwa na dunia, kabla ya kuingia zizini mwa Bwana. Wengine wanapanga kungoja mpaka wawe wazee ndiyo waje kwa BWANA, kwa vile mshahara wao utakuwa sawa na yule aliyeanza mapema. Hili ni kosa, kwani hatujui maisha yetu yatakoma lini. Na hatujui huzuni zitakazotupata duniani tukiwa makafiri, kisha tuwarithishe watoto wetu ukafikiri kabla ya uzee wetu. Tuje mara tunaposikia sauti ya Mungu ikituita, na tukae shambani kwa furaha, wala tusiwe na wivu na kujilinganisha na wanaokuja baadaye. Tusidhani uzoefu wa mwizi wa msalabani, aliyemwamini Yesu alipokuwa anakaribia kufa unaweza kuwa uzoefu wetu pia. Watu hawa wanaopeleka uamuzi mbele kwa kusema kesho kesho, mara nyingi wamepata shida nyingi wakiumizwa na maisha waliyoishi bila kumjua Yesu bali walikuwa wakitembea kwenye kivuli cha Shetani. Hatutatamani vile walivyoburuzwa na kutaabishwa hata kuumizwa. Sisi tukae kwa BWANA tutazame uzuri Wake leo, kuanzia leo, na saa hii hii na hata milele. Ndilo ombi langu, Je! Hili pia ni ombi lako? Basi tujiunge kuombeana, na kualika wengine pia waingie katika safina, wakati misumari ya mwisho inapigwa!

**Yaweke mahitaji yako, furaha yako, huzuni yako, wasiwasi wako, na hofu yako mbele za MUNGU. Hauwezi kumlemea Yeye; huwezi Kumchosha. Yeye anayehesabu nywele za kichwa chako hapuuzii yahusuyo mahitaji ya watoto Wake. “Bwana amejaa huruma na rehema” (Yakobo 5:11). Moyo Wake wa upendo unaguswa na huzuni zetu na hata tunapozitaja Peleka Kwake kila kitu kinachototatanisha akili. Hakuna kitu kikubwa mno kwake kitakachomshinda kubeba, kwani Yeye anashikilia ulimwengu. Anatawala juu ya mambo yote ya ulimwengu.
-------------------------

Maswali: Mshahara katika kisa hiki ni nini? Watu waliokuja asubuhi kwenye kisa hiki wanawakilisha nani? Kwa nini wa kwanza watakuwa wa mwisho na wa mwisho watakuwa wa kwanza? Je Kwa nini watu wanaona wivu Mungu akiwabariki wengine? Je! Tunaweza kuondoaje wivu kwa wengine wakifanikiwa?

**SIKU YA 253.**
**(Septemba 9)**

# Kukaa mkono wa kuume au kushoto mbinguni.

**Mathayo 20, Marko 10.**

Yesu akatabiri tena kifo Chake kwa mara ya tatu akisema, Tunapanda Yerusalemu, na mambo yote, Mwana wa Adamu aliyoandikiwa na manabii yatatimizwa. Kwa kuwa atatiwa mikononi mwa mataifa, wakuu wa makuhani na waandishi, Naye atafanyiwa dhihaka; atatendwa jeuri, na kutemewa mate; nao watampiga mijeledi, kisha watamwua; na siku ya tatu atafufuka. Wanafunzi hawakuelewa Maneno hayo hata kidogo, na jambo hilo lilikuwa limefichwa kwao. Wao walikuwa wanafikiria jinsi ambavyo wangekuwa mawaziri, au makamu wa Raisi baada ya kuwaondoa Warumi na jinsi Yesu atakavyosimika serikali, nao watakavyokaa kwa raha mstarehe.

Baada tu ya Yesu kuwaambia atateswa na kufa, wao vado waliendelea na mjadala walioupenda wa ubwana ukubwa watakaopata karibuni; wasijue kwamba Yesu akifa kama alivyotabiri, ndiyo utakuwa umewadia wakati mgumu wa kushuhudia wengine, kupata dhiki kubwa na hata kuteswa. Wakazungumza na mama yao yaani mama Salome Zebedayo au Mrs Zebedayo. Pengine waliona Yesu atamsikiliza mama yao kwa kumheshimu na kisha awape vyeo. Hata hivyo mama huyu alijitoa kwa Yesu pia, akitumia hazina zake. Kwanza Yesu alikuwa na watoto wake wawili wenye nguvu na usongo.

Mama huyu na mume wake watakuwa walimsaidia Yesu na mitume, kwa hali na mali maana watoto wao walimpenda Yesu mpaka wakaacha kila kitu. Mama huyu aliruhusu watoto wake watembee na Yesu, nao wakabaki hawana wa kuwasaidia nyumbani. Huku kulikuwa kujitoa kwa hali ya juu. Sasa alitaka Yesu awalipe vijana wake kwa kuwapatia vyeo. Je, wewe usingepende mtoto wako atunukiwa na Masihi? Ni kweli walimpenda Yesu na wakamuunga mkono, na walipenda kumsikiliza, isitoshe kwa utamaduni ule kama Afrika, mama ya mitume alikuwa mama kwa Yesu pia, maana walikuwa marafiki Zake. Huenda hawa vijana walimpanga mama yao aseme maneno hayo kwa Yesu, au ulikuwa mpango wa huyu mama mwenyewe wa kutoka moyoni mwake, kwani kila mama hupenda watoto wake wafanikiwe au wawe katika madaraka ya juu, asijue madaraka ya mbingu ni tofauti na ya dunia.
Basi mama wa Yohana na Yakobo, wana wa Zebedayo akaja akamsujudia Yesu akimwambia anataka amwombe jambo fulani, Yesu akasema "wataka nini?" Naye akamwomba Yesu aagize wana wake wawili yaani Yakobo na Yohana mmoja akae mkono wa kushoto Kwake na mwingine mkono wa kuume Kwake "kwenye ufalme wako." Naye Yesu akasema akiwa na uso wa makini "hamjui mnaloliomba", Je wanaweza wana wako kunywea kikombe nitakachokinywea au kupata mateso au dhiki nitakazozipata? Nao wakasema kwa ujasiri "tunaweza" Naye akawaambia mtakinywea kikombe Changu, lakini kuketi kuume au kushoto kule mbinguni "sina amri kuwapa bali watapewa waliowekewa tayari na Baba Yangu."

Sidhani kama kuna mtu anayeweza kukinywea kikombe cha Yesu maana hakuna mtu anayeweza kufanya yale aliyoyapitia. Sisi kama binadamu twaweza kupata mateso, ila kama tungekuwa tuna uwezo tungeepuka. Yaani kama binadamu, mtu angetutundika msalabani, na tuna uwezo wa Kiungu/Mungu kutoka, tungetoka na kuacha watu midomo wazi pale Golgotha. Pengine tungefanya miujiza na kuwafanya watu wanaotusulubisha wapooze mwili pale pale, ili wasiweze kupiga misumari. Hata hivyo mzigo wa Yesu ulikuwa tofauti, ulikuwa ndani ya moyo, akibeba dhambi na huzuni za dunia yote, watu zaidi ya bilioni 10 waliowahi kuishi katika miaka 6000 ambayo dunia imekuwako. Mzigo huu ni  Mwana-kondoo wa Mungu tu mwenye uwezo wa kuubeba. Kwa sababu hiyo, ni Yeye tu Ndiye anastahili, kukaa kuume kwa BABA. Sisi hatuwezi hata kubeba huzuni za watu wa karibu yetu, na hata kama tunaweza huwa tunakwepa.

Wanafunzi wengine waliposikia wenzao wanachotaka, japo nao pia wazo hilo lilikuwa limewapitia, waliwakasirikia Yohana, Yakobo na mama yao. Walikasirika kwa vile nao walitaka nafasi hizo, na kuzifanyia kampeni, ni vile hawakuwa na ujasiri wa kusema au kuleta wazazi wao.  Ndipo Yesu akawaambia, wafalme wa mataifa hutawala kwa nguvu na wakubwa wao hutumikisha watu. Hakupinga mtu kuwa na madaraka, ila alifafanua kuwa kwenye ufalme wa mbinguni viongozi ni watumishi wa watu na si wanyapara. Anayetaka kuwa mkubwa, ni lazima awe mtumishi wa watu, na anayetaka kuwa wa kwanza na awe mtumwa. Maana hata Yeye hakuja kutumikiwa bali kutumika na kutoa nafsi yake kuwa fidia ya wengi. Basi yeyote aliye mkubwa apaswa awe mdogo. Wazazi wengi wanahitaji hekima ya jinsi ya kusaidia watoto wao kutatua matatizo  yanapowajia, hebu wazazi wapewe  hekima ya kuwafundisha watoto wao vitu vya kuweka kipaumbele. Mama Zebedayo angekuwa na hii hekima, asingesikiliza yale ya watoto, bali angewapa ushauri bora.

Madaraka hata yawe madogo kiasi gani, yana kawaida ya kuharibu tabia za wengi. Hayo ndiyo yalimwangusha Shetani mbinguni, japo alikuwa juu tayari, alitaka kuwapindua wengine waliomwumba aendelee kupanda juu. Wengi wakiwa kwenye madaraka hughafilika, wakitaka watu wawaabudu, wawasujudu, wawasihi na kuwalilia, wakisahau pale Mungu alipowatoa walipokuwa hawana kitu. Yesu ametupa mbinu hata leo kwamba tukitaka tuwe wakuu lazima tuwe watumishi, na aliye wa kwanza atakuwa wa mwisho na wa mwisho atakuwa wa kwanza. Sasa ukitaka uwe chini kwa makusudi uwekwe juu utakuwa umepoteza lengo. BWANA anauona moyo. Yesu alikuja kutoa maisha Yake kwa kufa kwa ajili yetu, na si kutafuta ukubwa, na tunapaswa kuwa na nia hiyo iliyoelezwa kwenye sura ya pili ya Wafilipi, soma sura hiyo tafadhali!

Toka udogo wetu tunafunzwa kufanya mashindano ya masomo, kukimbia, au kutafuta pesa, na mambo mengine, ila kumbuka tukitaka kuwa wa kwanza kila mahali na kuwa na roho ya mashindano, tunakuwa na mawazo ya kujifikiria na kujidanganya. Tabia za namna hii hazina nafasi mbinguni. Pale ni mahali pa kufikiria wengine na kuwapenda na si kuona jinsi tunavyoweza kuwapunja au kupata faida kuliko wengine, au kuwa bora kuliko wao. Jambo hili ni la kuangaliwa hata kwenye michezo, michezo yapasa kutusaidia mazoezi, na kujenga urafiki, na kupata mbinu za kutatua matatizo, na si roho ya ushindani au chuki, au kushabikia michezo kuliko

maisha yetu ya kiroho.

*Omba kwa Imani; Kisha Pokea — Kuna nguvu inayopatikana kutoka kwa MUNGU. Anaweza kusaidia. Anaweza kutoa neema na hekima ya mbinguni. Kama utaomba kwa imani, utapata; lakini ni lazima ukeshe katika maombi. Kesha, omba, fanya kazi, ndiyo inapaswa kuwa kauli mbiu yako


------------------------

Mama Yohana na Yakobo alikuja na ombi gani? Yesu alimjibuje? Formula ya ukuu ni nini? Je, ni kweli wanafunzi wangeweza kukinywea kikombe cha Yesu? Je mtu akiwa mtumishi wa watu huku akiwa na nia ya kutaka ukubwa itakuwaje?

**SIKU YA 254.**
**(Septemba 10)**

# Kipofu Batimayo.

**Mathayo 17. Luka 19**



Muda ulikuwa unakwisha, na Yesu alijua hili, na alipokuwa na mitume peke yake alijaribu kuwakumbusha kwamba juma hili yale maisha ya furaha waliyoishi, yatakuwa yakifikia mwisho wake. Bahati mbaya hawakumwamini, aliposema kwamba lazima aende Yerusalemu na atapata mateso kutoka kwa wazee, wakuu wa makuhani na waandishi na kuuawa, kisha atafufuka siku ya tatu. Wao waliona yote haya hayawezekani. Kwa nini kijana wa miaka 33 atake kuhatarisha maisha yake, wakati ambao hata wao wengine waliokuwa na umri mkubwa kwa Yesu walitaka waishi zaidi? Kwa nini asitoroke ili asaidie miji na hata nchi zingine walio na shida? Hata Petro alikuwa ameshamgombeza kwamba hayo hayawezekani.

Mambo yote yalikuwa yameenda sawa, na miujiza ilifanya wengi wamsikie; chakula walipewa, na wakafurahi na kushiba. Je makuhani wataharibu haya yote, wakati walikuwa tayari alete ufalme duniani na kuwafukuza Warumi? Haikuwaingia mawazoni mwao, kwamba kama Yesu ni Mwana-kondoo wa Mungu kama vile Yohana alisema, hivyo basi yapaswa atolewe kafara. Ingekuwa rahisi kwa Yesu kujificha, kama angetaka kufanya hivyo. Angeenda India, Australia au angekuja Afrika tena, kama alivyoenda Misri. Ila Yesu hakukimbia kwa ajili ya mateso aliyojua kwa undani yanakuja. Je, unajua ni kwa nini Yesu hakukimbia?

Wakielekea mjini Yerusalemu, jioni ilifika wakiwa kijiji cha Wasamaria. Yesu akawatuma Yohana na Yakobo, wale wanandugu waende wakaulizie nyumba ya wageni au hoteli ya kulala usiku ule. Wanafunzi hawakuona shida, maana alikuwa amekaa Samaria, siku za nyuma akisaidia wengi na kuhubiri kule, wakafikiri wangempapatikia akae kwao. Walijua Yesu alipenda Wasamaria kama alivyowapenda Wayahudi. Hata hivyo walipouliza uwezekano wa kupata mahali pa kulala walikataliwa. Walipotaka kujua sababu waliambiwa "Kwa sababu BWANA wenu anaelekea Yerusalemu." Hii ni kama sheria iliyokuwepo siku hizi 'Rais wa nchi akienda kutembelea nchi fulani, hawezi akaunganisha matembezi yake na nchi ambayo ni ya uadui na nchi hiyo

katika msafara ule; bali yabidi arudi nchi yake, na aanze tena safari kuelekea nchi ya adui'.

Mitume wakapata ghadhabu, na wale kaka wawili, 'wana wa ngurumo wakampa Yesu ushauri "Je unataka tuagizie moto toka mbinguni uwale hawa Wasamaria kama vile Eliya alivyofanya kwa manabii wa Baali kule mlima Karmeli?" Yesu alishangaa hii roho ya ghadhabu na hasira ya namna ile. Je umepata hasira watu wanapokuudhi, ukataka wapotee usiwaone tena milele? Hata leo wengi wana pepo la hasira, wakifikiri wana haki ya kuwa na hasira, yaani ghadhabu ya haki, hilo ni kosa. Hasira ina nguvu kali mioyoni mwetu, na kila mtu anaipata, tumwombe Mungu atuondolee pepo la hasira. Watoto na watu wazima tujifunze kuondoa hasira, maana ni dhambi. Yesu aliwajibu mitume "Mwana wa Adamu hakuja kuangamiza maisha bali kuyaokoa." Kutamani kuwaumiza wengine ambao hawaafikiani na yale tunayowaambia ni kazi ya Ibilisi, kamwe usimwumize mtu anayeipinga imani yako, wacha Mungu amshugulikie.

Yesu Akaangalia kile kijiji kilichowafukuza, akawaonea huruma, maana alikuwa anaenda Yerusalemu kufa kwa ajili yao na sisi sote binadamu, nao wasijue kinachoendelea. Jazba, malumbano, ubaguzi wa makabila au dini, na wivu vililikuwa vimewajaa. Hata leo wewe, Je una ubaguzi uliojengwa juu ya kabila lako au dini yako. Basi kama ni hivyo, Yesu anakuita umkaribishe kwako au uwakaribishe watu Wake? Siku za mbele Wasamaria walipomkaribisha Filipo ahubiri, kipindi kile baada ya Yesu kupaa, pengine waligundua nafasi nzuri waliyopoteza kumkaribisha Mwana wa Mungu na kumpa faraja moyoni Mwake kabla ya kuiendea huzuni yake kuu. Yesu hakukasirika bali alienda kijiji kingine, hatujui ni kipi, ila twajua walibarikiwa kule alikopokelewa.

Yesu alijitahidi kuwaeleza mambo yanaoenda kutokea, ila walichukua muda kuelewa. Japo walishangaa Wasamaria wanawafukuza, hawakufikiria Wayahudi waliokuwa wanaenda kumwua juma hilo, bado waliona Wasamaria wana shida zaidi. Walikuwa wametafsiri unabii kwa makosa, wasitake kufundishwa, au kubadilika. Hawakujua ushindi wa Yesu na wetu binadamu utatokana na kifo Chake, na kufufuka Kwake. Wao waliona kifo ndiyo kushindwa kwa mwisho. Juma hili lilikuwa kilele cha pambano la shetani na Mungu. Shetani alikuwa anaenda kushindwa kwa kiwango cha juu kuliko mara zote. Yesu aliwakumbusha kwamba wana Nuru kwa muda waitumie Nuru hiyo, giza lisije likawashinda.

Wakitoka kwa mama Yohana na Yakobo, mkutano mkubwa ukamfuata Yesu na vipofu wawili ambao walikuwa omba omba, mmoja akiitwa Batimayo walikuwa wameketi kando ya njia nao waliposikia Yesu anapita walipaza sauti wakisema "uturehemu, BWANA Mwana wa Daudi." Mkutano ulichoka na kero zinazosababishwa za kelele za vipofu hawa kwasababu wao walikuwa na macho tayari. Hata hivyo wao walikuwa hawana shida, waliona kuwa wanalolifanya ni jema na kusahau kuwa ni kero kwa wengine. Vipofu hawa hawakuchoka, bali walizidi kupaza sauti, wakisema "uturehemu BWANA, Mwana wa Daudi!" ndipo Yesu akasimama na kuwaita. Watu wakawaambia wale vipofu "jipeni Moyo Yesu anawaita." Wakatupa mavazi wakaruka wakaenda kwa Yesu; Naye akawauliza "niwafanyie nini?", nao wakasema

shida yao “macho yetu yafumbuliwe.” Yesu alijua shida yao, ila alitaka waseme wenyewe.

Yesu akawaambia “Enendeni zenu, imani yenu imewaponya”, mara wakapata kuona nao wakamfuata njiani. Hata leo tunasali, japo Mungu ajua shida zetu tunamwambia, hili linatusaidia mioyoni, kwani tunazungumza Naye kama rafiki. Naye anapenda kusikiliza sauti za watoto Wake! Yesu akawahurumia vipofu, na akawagusa macho yao, na mara wakapata kuona. Akawaambia Enendeni zenu, imani yenu imewaponya, mara wakapata kuona na wakamfuata njiani, wakimtukuza Mungu na kumsifu. Vipofu wakaanza kuzuru sehemu mbali mbali waone mambo mapya, waliyokuwa hawajawahi kuona. Wakavishika walivyovisikia, na kuvitazama. Hakika maisha yao yalibadilika kabisa.

Vipofu walikuwa kama watoto kwani waliona hawawezi kujitumaini wenyewe, na wakamtegemea Mungu kabisa, ambaye walijua ndiyo pekee atakayewatoa kwenye shida ya upofu wao wa macho. Yeyote yule anayemtumaini Mungu kama mtoto, ndiye mkuu mbele za Mungu.

*Usizimie nguvu ikiwa Hakuna Jibu La Mara Moja lililotolewa — Imani yako haipaswi kuachilia ahadi za MUNGU, ikiwa hautaona au kuhisi jibu la haraka la maombi yako. Usiohofu kumtumaini MUNGU. Zitegemee ahadi Zake za kweli: “Ombeni, nanyi mtapewa.” MUNGU ni mwenye hekima mno kukosea, na ni mwema sana kuwazuilia watakatifu Wake wanotembea katika unyoofu kitu chochote chema.
---------------------------

Maswali: Wayahudi walitafsirije unabii wa Masihi kwa makosa? Kwa nini Yesu hakujificha au kukimbilia Uyunani? Kwa nini kijiji cha Samaria kilikataa Yesu asiingie kwao? Ujasiri wa Batimayo unatufundisha nini?

**SIKU YA 255.**
**(Septemba 11)**

# Kulipa kodi ni halali.

***Mathayo 22 na 24.***



Ilikuwa sheria ya Musa kila mtu aliyepita miaka 20 kulipa nusu shekeli maalumu iliyoitwa Drakma. Hii waliichenji au kuipata hekaluni ili watoe kodi. Walipofika Yerusalemu, wanafunzi na Yesu; wale watozao ushuru wa nusu shekeli walimwendea Petro na kuuliza, Je mwalimu wenu hatoi nusu shekeli? Akasema “hutoa.” Alisema hivi bila ya kufikiria mno ule mtego wa Wayahudi. Naye alipoingia nyumbani Yesu alimwuliza “Waonaje Simoni Petro, wafalme wa dunia hutwaa kodi au ushuru kwa watu gani? kwa watoto wao au kwa wageni?” Petro akamjibu, “hutoza ushuru wageni, Naye akasema kama wanawatoza wageni kodi basi wana wako huru.

Lakini ili wasije wakawakwaza Wayahudi, Yesu alimwambia Simoni aende kutupa ndoana baharini na kutwaa samaki, na akifumbua kinywa chake samaki azukaye kwanza, ataona shekeli, na hiyo achukue na kulipa kwa ajili yao. Wayahudi walitaka kuona kama Yesu analipa kodi ili waibushe malumbano mengine, maana makuhani, na manabii hawakupaswa kulipa; Yesu asingelipa wangetaka wampeleke kwenye mamlaka, ila angelipa wangesema, basi ‘wewe si nabii’. Yesu alipata shida na utawala wa kanisa kuliko utawala wa Rumi. Hakuna mahali tunasoma, waliposema

utawala wa Rumi walikuja na kumtega kwa hili au kwa lile. Hata katika kupindua meza, Yesu hakwenda kupindua meza za ikulu au za kwenye maofisi ya serikali bali kwenye hekalu, maana hapo ndipo palijaa hila, na akajua kwamba watu wa hekaluni wangeacha uovu wao, hata serikali iliyotawala ingebarikiwa na kumwamini Yeye kirahisi.

Petro alivyogundua mtego wao, akajua kwamba ingekuwa vyema angesema "Mwalimu wangu halipi kwa vile Yeye ni Mwana wa Mungu." Yesu alijua jinsi ya kupata sarafu ya hekalu "drachma" na akajua ni samaki gani atakuwa nayo. Mfano huu ni mzuri hata kwetu leo, badala ya kupoteza muda kubishana na watu kwa mambo madogo, ni vyema tupange muda wetu kushuhudia wengine, na kuwasaidia wenye mahitaji.

Siku nyingine mafarisayo wakitaka kumtega Yesu ili wamshike. Walimtumia mafarisayo vijana wenye akili nyingi na maherodi wakisema "Mwalimu twajua ya kuwa U mtu wa kweli, na njia ya Mungu waifundisha katika kweli, wala hujali chochote cha mtu awaye yote, kwa maana hutazami sura za watu, tuambie, waonaje? Ni halali kumpa Kaisari kodi, ama sivyo? Yesu akijua mioyo yao ina hila na wanataka kumjaribu ili aingie mtegoni na serikali kwamba anawapinga, au halipi kodi aliwajibu "mbona mnanijaribu enyi wanafiki?" akawaamuru walete dinari au ile fedha ya kodi, nao wakamletea.

Akawauliza sanamu na anuani au nembo kwenye sarafu ni ya nani? Wakamwambia ni ya Kaisari ambaye ndiye alikuwa anatawala wa nchi hiyo wakati ule. Naye akawaamba "Basi mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari na Mungu yaliyo ya Mungu." Waliposikia walistaajabu wakamwacha na kwenda zao. Ili serikali imudu kuendesha huduma na shughuli zake, inahitaji kodi. Kodi kwa serikali inayotenda haki, yatumika kujenga barabara, kukarabati mahospitali, kulipa walimu, kujenga mashule na mambo mengine ya maendeleo. Serikali kwa kawaida inategemea raia wake kuiendesha. Nayo serikali inapaswa kutokuwa na ubaradhifu wa mali za raia, hii ni dhambi na uhalifu pia.

Kuna baadhi ya serikali za dunia zinatoza kodi na kuumiza raia kwa kutumia pesa hizi kwa manufaa yao tu; ila mpango wa kodi toka awali ulikuwa kwa matumizi mazuri. Hata hivyo serikali ni watu wenyewe, hivyo mara zingine tusiulize serikali itatufanyia nini, bali hata sisi 'tutaisaidiaje serikali yetu'. Cha muhimu kingine ni kuiombea serikali na viongozi wote ili kila siku ili kuweze kuwa na amani ili hata kuabudu kuwe bila mateso. Tukumbuke mtu anayempenda Mungu ni raia wa nchi mbili, mbinguni na duniani.

Kutoa sadaka na kurudisha zaka ni muhimu, maana tunarudisha kidogo sana ukilinganisha na mengi ambayo BWANA anatukarimia. Mungu ametuachia tutoe Kwake, kwa hiari, hatutaenda gerezani tusipozitoa kama serikali inavyofanya, bali tutapoteza baraka kubwa, kwani ni Yeye Ndiye mtoaji wa yote, iwe familia, mahitaji, afya au mali. Kama unafikiri unampa Mungu kuliko anavyostahili, Yeye si dhalimu atakurudishia chenji, na kukupa bakshishi au bonasi.

*Ni fursa yetu kuomba kwa ujasiri, Roho akichochea maombi yetu. Kwa unyenyekevu tunapaswa kuelezea mahitaji yetu kwa Bwana, na kudai ahadi Yake.

*MUNGU Kawaida Hajibu Maombi Asiyoulizwa — Maombi na Imani vitafanya kile ambacho hakuna nguvu yoyote duniani inaweza kutimiza. Ni nadra sana, katika hali zote, tunawekwa katika nafasi ile ile mara mbili. Tunakuwa na matukio mapya na majaribu mapya ya kuyashinda, ambapo uzoefu wetu wa zamani hauwezi kuwa mwongozo wa kutosha. Lazima tuwe na nuru siku zote inayotoka kwa MUNGU. Kristo daima hutuma ujumbe kwa wale wanaosikia sauti Yake.
------------------------------

Maswali: Yesu alilipaje kodi? Kwa nini Yesu alilipa kodi? Watu gani walimfuata Yesu kumtega na maswali? Yesu aliwajibuje? Kwa nini kurudisha zaka na kutoa kodi ni muhimu kwetu leo?

**SIKU YA 256.**
**(Septemba 12)**

# Twapasa kusamehe watu kama Mungu anavyotusamehe.

**Mathayo 18**



Je mara zingine dada, kaka au marafiki zako wanakuchokoza, na unashindwa kuvumilia, au kuwasamehe? Je mara zingine unataka uwasengenye na kuwaambia watu wengi wajue jinsi walivyo wabaya? Pengine umeuliza “Mbona sina ruhusa ya kukasirika na kuacha kumsamehe mtu anayeonekana amenikosea kabisa.” Si wewe peke yako unayefikiri hayo. Binadamu wote, tukichokozwa au kuumizwa inachukua muda kusamehe au kusahau. Je, Yesu alipofanyiwa mabaya na watu alifanyeje? Petro alimwendea Yesu na kumwuliza “ndugu yangu anisamehe mara ngapi nami nikubali kumsamehe? Je, nimsamehe mara saba? Petro alifikiria mara saba, ndicho kiwango kinachotosha ambacho mwanadamu anaweza kustahimili. Akashangaa atakumbuka kuhesabu haya, na kuweka kumbukumbu.

Yesu akamwambia si mara saba, bali hata 7 x 70, ambayo ni 490! Petro akashangaa atakuwa anahesabu hizi nambari na kukumbuka rekodi zake, kwamba sasa ni mara ya 233, 234, 235, 236 mtu amenifanyia makosa, na huyu ni mtu mmoja. Mwingine pia ana rekodi, amemkosea mara 472 na mwingine 15, kisha kuna wengine watano wamebakia, nao wana namba zao walizosamehewa. Hesabu inaendelea kuchanganya ubongo na kuleta msongo! Yesu alijua hakuna anayeweza kutunza

rekodi hiyo, na hakutaka tuitunze rekodi ya namna hiyo. Isitoshe watu wangapi wametukosea mara 490 kwa siku moja? Ni vigumu kukosewa mara hizo. Kama yupo mtu anayetukosea jambo moja kila siku basi itakuwa zaidi ya mwaka kufikisha hizo mara 490.

Je umeshawahi kukosewa na mtu mara hizo 490? Kama La! chukua daftari na orodhesha wale wote ambao una hasira nao, na yale waliyokutendea, na makosa hayo wameyatenda mara ngapi, kisha mwombe Mungu ili uwasamehe, maana kusamehe watu ni zawadi inayotoka kwa Mungu. Nafikiri ukifika kama namba 20 utakuwa umesahau, yote waliyokutendea na mtakuwa marafiki tena. Jaribu uone, jinsi mpango wa Mungu wa kusamehe ulivyokuwa wa kutoka mbinguni. Yesu alikuja atuonyeshe hilo, ili tusiangamie; maana kutosamehe watu kumewaingiza baadhi yetu kwenye dhambi ya chuki. kiburi, na wivu hata wengi wataangamia milele kwa dhambi hii. Je, kweli uovu wa mtu mwingine, utufanye sisi twende motoni? La! hasha roho ya kusamehe na kutoa kinyongo haiji kirahisi kwa binadamu yoyote, ni mapigano ya moyo.

Yesu alimaanisha tuwasamehe watu mara zote, yaani hakuna mpaka wa kusamehe. Twaweza tusiwe na mahusiano nao ya namna fulani baada ya kuona tabia fulani, ila yapasa tuwasamehe na kujitahidi kurudisha mahusiano mema nao. Mfano kama mtoto anakuazima penseli kila siku na kupoteza, msamehe, ila siku nyingine anapokuja, ukiwa na penseli ya ziada mpe tu kama zawadi, usimwazime, ila kama huna uwezo wa kununua nyingine usimwazime, mwambie kwamba kwa kweli hilo halitawezekana kwani hana kawaida ya kurudisha anapoazimwa. Ila kwa zile penseli alizoazima na asikurudishie, msamehe. Ukristo ni zaidi ya kutunza amri za Mungu. Sala ya BWANA yasema tunasamehewa tu pale tunaposamehe.

Yesu akaendelea kutoa mfano wa ufalme wa mbinguni, akisema, umefanana na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake. Alipofanya aliletewa mtu mmoja mwenye deni la talanta 10,000. Naye akakosa cha kumlipa yule Bwana wake, na masharti yakawa auzwe yeye, mke na watoto wake na vitu vyote alivyo navyo, ili ikatumiwe kulipa lile deni. Jambo hili la kuwa mtumwa ni la kutisha maana kuwa mtumwa ni kufanya jinsi bosi au bwana anavyotaka. Yule mtumwa alipofikiria shida itakayowapata mke na watoto wake, alianguka akimsujudia yule Bwana na kumsihi “nivumilie, nami nitakuja kukulipa yote pia.” Yule Bwana wa mtumwa akamhurumia, akamfungua toka kifungoni na kumsamehe lile deni.

Mtumwa yule alitoka gerezani kwa furaha, na akiwa njiani alimwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia tu. Akamkamata na kumkaba koo na kumfanyia ukatili, akisema “nipe deni langu.” Yule mjoli aliangaka miguuni pake na kumsihi amvumilie naye atamlipa yote. Ila huyu bwana aliyesamehewa talanta 10,000 hakutaka kusikia, bali akaenda na kumtupa yule mjoli kifungoni, hata atakapolipa deni lile la talanta 100. Wajoli wengine walipoona hili walisikitika sana, maana walijua tajiri wake alishamsamehe mtu huyu, wakaenda kumweleza bwana wao yaliyotendeka. Ndipo yule Bwana akamwita yule mtu aliyekuwa amesamehewa na kumwambia “Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi, nawe Je haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe?”

Bwana yule alighadhabika sana kwa kuona uonevu, na kujipenda alikofanya huyu bwana aliyekuwa na deni kubwa, akampeleka kwa watesaji hata atakapoilipa lile deni lote.

Yesu akasema hata Mungu mbinguni, atatenda vivyo hivyo, "msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake." Tunasamehewa tukisamehe wengine, maana nasi Mungu anatusamehe, hebu tusiwe na kiburi kwamba sisi hatuwezi kukosewa. Mara nyingine ni vigumu kuwasamehe watu waovu. Hili linawezekana kwa kumwomba Mungu maana, mara nyingi tunakuwa na maumivu mtu akitufanyia maovu, ila tujifunze kusamehe. Ni nani asiyemkosea mwenzake, au asiyehitaji kusamehewa? Mtu asiyesamehe anakuwa mtumwa kwani anabeba kisasi au chuki, na inakuwa kama amekula sumu akitegemea yule aliyemtendea uovu ndiye atakufa. Kutosamehe kunatuondolea raha yetu na kutufanya tuwe vifungoni. Watoto wadogo husamehe kirahisi, na hili ni fundisho kwetu watu wazima.

Baba yetu wa mbinguni ni kama yule mfalme aliyemsamehe yule mtenda kazi deni kubwa. Ana huruma na ni mkarimu sana kutusamehe dhambi zetu. Anategemea nasi tutafanya vile vile, kwa maana ametupa mfano. Kuwa na roho ya kusamehe ni kitu cha thamani mno, kuliko pesa, ndiyo maana Yesu alisema hata kama tuna mamilioni ya pesa tunaenda kutoa sadaka, tuziache kutoa zile sadaka kisha twende tukapatane na wale tumewakosea au wametukoesa. Tukumbuke tunasamehewa tu pale tunaposamehe wengine.

Yesu akazungumzia kuhusu mahusiano ya watu. Mtu akikukosea ufanyaje? Alizungumza haya alipozungumza kisa cha mtu mwenye kondoo 100 na mmoja akipotea huacha wote 99 na kwenda kumfuata huyo mmoja. Kisha akasema "Ndugu yako akikosa, enenda ukamwonye, akikusikia umempata nduguyo. La! kama hakusikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike. Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asiposikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru.

Yaani mtu ambaye hamjui Mungu, anayehitaji kuambiwa tena habari za Mungu, ili amwamini tena, kwani amerudi nyuma kiimani. "Amini nawaambia yoyote mtakayofunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni na yoyote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni. Tena nawaambia ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lolote watakaloliomba watafanyiwa na BABA Yangu aliye mbinguni. Kwa kuwa walio wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, Nami nipo papo hapo katikati yao."

Hivyo tusipuuzie mambo ya pamoja, si kwamba tukiomba peke yetu hatusikiwi, bali kutokana na ahadi ya Biblia kuwa pamoja pana nguvu zaidi. Hata kule mbinguni, hatutaishi peke yetu, sisi ni watoto wa baba mmoja, Bwana anasema amri ya pili kuu ni sawa na ile ya kwanza. Je, unajua amri ya pili kuu katika ya zile mbili, inasemaje?

*Dawa ya Kukata Tamaa au kufa moyo Ni Imani, Maombi, na Kazi — Kwa wale wote waliokata tamaa kuna tiba/dawa moja tu, - imani, sala, na kazi.

--------------------------

Maswali: Kwa nini Yule mtumwa aliyesamehewa alikataa kumsamehe mwenzake? Petro aliuliza swali gani? Je ni mara ngapi Yesu alisema Petro asamehe? Je Kwa nini tusiposamehe tutakuwa utumwani? Je huyu mtu mkatili asiyasamehe anakufundisha nini? Mtu aliyepoteza kondoo anamwakilisha nani?  Je kuna idadi ambayo twaweza kufika na kuacha kusamehe? Kwa nini ni muhimu kujua watu walioumizwa huumiza wengine na hivyo tujifunze kuchukuliana nao na kuwasamehe upesi?

**SIKU 257.**
**(Septemba 13)**

# Hosana mbarikwa ajaye kwa Jina la BWANA.

**Mathayo 21**



Muhtasari wa juma la mwisho la Yesu kabla ya kufa.

1. Jumapili: Alipanda punda na kuingia Yerusalemu.
2. Jumatatu: Akafukuza watu kwenye hekalu na kukausha mtini.
3. Jumanne: Alifundisha hekaluni.
4. Jumatano: Yuda aliendа kumsaliti. Mariamu alimpaka Mafuta.
5. Alhamisi: Kula mkate/divai pamoja, mafundisho ya mwisho na kuomba bustani ya Gethsemane.
6. Ijumaa: Yesu akamatwa, atuhumiwa na Sanhedrin, ahukumiwa kufa na Pilato
7. Ijumaa: Yesu afa msalabani, na kuzikwa.
8. Jumamosi: Yesu apumzika kaburini
9. Jumapili: Yesu afufuka na kuwatokea Mariamu, wanafunzi wa Emmausi na wanafunzi Wake.

Basi juma la mwisho la Yesu, duniani alikuwa akitembea kutoka Efraimu, kukaribia Yerusalemu na kufika Bethfage, katika mlima wa mizeituni. Yesu alisimama na kutuma wanafunzi Wake wawili "enendeni kijiji kile kinachowakabili, na mara mtaona punda amefungwa, na mwana-punda pamoja Naye; wafungueni mniletee. Na mtu mmoja atawauliza, ni nini kinachoendelea, basi mtamwambia "BWANA anawahitaji na mara huyo atawapa."

Walishangaa kidogo, maana kilikuwa kitu cha ajabu kwao kwamba alijua hata umri wa punda! Haya yote yalikuwa litimie Neno lililonenwa na nabii Zekaria, akisema "mwambieni binti Sayuni; Tazama mfalme wako anakuja kwako. Mpole Naye amepanda punda, na mwana-punda mtoto wa punda" wakafikiria wanafunzi. Mfalme wa Wafalme, alikuwa mnyenyekvu bila bendera wala mapambo. Serikali zingine kama Uingereza hutumia dola 50 milioni kuwahudumia na kuipamba jamii ya mfalme. Yesu alikuwa amefanya kazi kwa mikono Yake, hakupanda magari ya fahari, bali alitembea kwa miguu. Watu matajiri walimpita na magari yao mazuri, ikiwemo na vumbi aliyoachiwa, ila Yeye alikaza moyo, akisema imempasa ahubiri kabla giza ya kuingia, wakati ambapo mtu hawezi kufanya kazi tena. Wale wanafunzi walienda wakafanya kama Yesu alivyowaambia. Pengine mtu huyu alikuwa mwanafunzi wa Yesu pia, basi wakamleta yule punda na mwana punda. Wakafikiria huenda wakati wa kuwa na maisha ya nafuu umefika maana siku zote walikuwa wakitembea kwa miguu na sasa wanaye punda.

Yesu akampanda punda, na watu wakaweka nguo zao juu ya punda, Naye akaketi juu yake, Punda akaanza kwenda. Ulikuwa wakati wa Pasaka, na watu wengi kutoka sehemu mbali mbali walikuwa wamekusanyika kusherekea pasaka. Vifijo na vigelegele vikatokea. Na makutano walipoona, nao wakatandaza nguo zao njiani na wengine wakakata matawi ya mitende na wakayatandaza njiani na kuyapunga. Hii ni sawa na vile watu wawekavyo zulia jekundu raisi wa nchi anapopita. Watu wakazidi kuongezeka na shangwe na nderemo zikazidi, huku sauti za furaha zikitanda anga kwa hiari ya moyo bila shinikizo la serikali au kanisa.

Makutano waliotangulia na wale waliofuata wakapaza sauti, wakisema "Hosana, Mwana wa Daudi; Ndiye mbarikiwa, Yeye ajaye kwa Jina la BWANA, Mfalme wa Israeli, Hosana juu mbinguni." Mafarisayo na makuhani walikasirika, ila walikuwa hawana jinsi. Naye alipoingia Yerusalemu, mji wote ukataharuki, watu wakisema, ni nani huyu? Makutano wakasema, Huyu ni Yule nabii, Yesu wa Nazareti ya Galilaya. Hakika Yeye alikuwa zaidi ya nabii, alikuwa Mwana wa Mungu. Yesu keshoye, akaingia ndani ya Hekalu tena mara ya pili, hekalu lilikuwa kama soko, au shamba la mifugo. Basi akawafukuza wote waliokuwa wakiuza hekaluni, akazipindua meza za wabadili fedha, waliokuwa wanabadilishia watu wapate sarafu maalumu ya kodi ya hekalu, iitwayo 'drakma/drachma'. Akavipindua viti vyao waliokuwa wakiuza njiwa. Watu walikuwa wameganda kwa mshangao, wala hawakuweza kufanya kitu. Akawaambia, imeandikwa, "nyumba Yangu itaitwa nyumba ya sala"; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyanganyi.

Vipofu na viwete wakamjia, Naye akawaponya, nao wakaendelea kumsifu kwa shangwe. Lakini wakuu wa makuhani na waandishi walipoyaona maajabu

aliyoyafanya na watoto waliopaza sauti zao hekaluni wakisema “Hosana, Mwana wa Daudi!” walikasirika, wakamwambia wasikia hawa wasemavyo? Yesu akinunuu Zaburi 8, akajibu “Naam; hamkupata kusoma Maandiko kwamba kwa vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao umekamilisha sifa?” Watoto hawa wasiponisifu, mawe yatapiga kelele yanisifu. Mitume walikuwa na siku ya furaha, kabla siku ya huzuni kuja juma lile. Pengine hata punda yule mdogo akafurahi kumbeba Muumbaji Wake, akafikiria amechaguliwa yeye, na wala si farasi, au tembo, isipokuwa yeye pamoja na udogo wake.

Yesu alikuwa mnyenyekevu, hakuchagua magari au vitu vya fahari kwa ajili ya usafiri. Tunajifunza kuwa leo tunapochagua magari au vitendea kazi tusitafute vilivyo vya gharama au vya anasa. Kama alivyokuwa punda, kwamba “BWANA anamhitaji”, hata leo kila mtu BWANA anamhitaji kutoa mwito wa mwisho wa habari njema za milele, kwa dunia ambayo inaenda kuangamizwa. Ombi la muhimu ni “BWANA kama unanihitaji, nionyeshe wapi, lini, na jinsi ya kukutumikia. Nisaidie nifanye unayotaka kwa uwezo wote, unaonipa, nitumie kufanya mapenzi Yako, leo mpaka siku ile nitakapokuwa nawe mbinguni milele.” Yesu alikuwa mfalme, bila ya askari, au silaha za kumlinda, ila wote waliomfuata walimfuata kwa kumpenda; hakuna aliyelazimishwa. Walimfuata kwa yale mema aliyowafanyia kwa upole, huruma na kujali. Wengine walikuwa wale walioponywa Naye; wakaonyesha furaha zao kwa dhati.

Ila wakashangaa Yesu aliposimama ghafula alipofika karibu na Yerusalemu, wengi wakakimbia wasikie anachosema. Naye Yesu alipouona mji akaulilia, Mfalme wa wafalme akalia, akisema “laiti ungalijua, hata wewe katika siku hii yakupasayo amani, maana yamefichwa machoni pako yatakayokutokea.” Watu wakashangaa, mfalme gani analia, wakati anasifiwa na kushangiliwa na watu, si afurahi basi? Yesu hakujililia Mwenyewe, bali alitulilia sisi, na wao. Ule mji ungekuwa na baraka na amani, ila ulikataa kuonywa. Yesu akaendelea kusema, kuna siku zitakuja ambazo adui “watakapokujengea boma wakuzunguke na kukuhusuru pande zote. Watakuangusha wewe na watoto wako na jiwe juu ya jiwe halitasalia. Yote yamekujia kwa kuwa hukutii ukasikia yale Mungu amekwambia ufanye.”

Haya yalitokea mwaka 70 BK wakati Tito Jemadari wa Rumi alipohusuru Yerusalemu. Machafuko ya namna hiyo yatatokea tena kwetu siku za mwisho pia. Walikuwa wamepata kiburi cha majengo mazuri, hekalu zuri mno la gharama, hivyo walijivunia. Watu hawakuweza kuamini kwamba hekalu lao zuri vile, siku moja litakuwa magofu. Yesu hakulilia majengo, bali alilia watu, maana wengi walikuwa wamemkataa kama Masihi, na adui watakapokuja kuhusuru mji, watoto na watu wazima watakufa, na hakuna jiwe litabakia pale, kwa sababu Yeye alikuja kuwaokoa nao wakamkataa, hivyo wengi kati yao watapotea milele. Yale aliyotabiri Yesu yalitokea baada ya miaka 50. Yerusalemu ikahusuriwa, sehemu iliyobaki leo ya hekalu lile la zamani ni ukuta tu. Soma kisa hicho kwenye kitabu kinachoitwa Pambano Kuu, ukikosa, tuandikie tukutumie!

Mahali pengi siku hii ya kuanza juma la pasaka inaitwa siku kuu ya matawi, na watu hutumia michikichi kwenye ibada. Wengine walifikiri ndiyo wakati Yesu

atakaposimikwa kuwa mfalme, wasielewe mambo magumu yatakayomfika Yesu, yaani kuuwawa juma lile kwa ajili ya dhambi zao na zetu mpaka mwisho wa dunia. Yesu alihuzunika, ndiyo maana alitoa machozi, kwamba wengi watapotea na kuangamia milele kwa kutokubali kafara Yake. Yesu alikuwa anajua Ijumaa ya juma hilo hilo, yaani siku nne zinazofuata; makuhani watamkamata na kumpeleka sehemu mbalimbali kwa kumdhihaki, na kisha kumtoa nje ya ukuta wa mji na kumpeleka Kalvari, ambapo watamwangika msalabani.

Je! Yesu angefanya mangapi kwa Yerusalemu endapo watu Wake na viongzi wangemkubali Yeye na upendo aliokuwa tayari kuwapa? Baada ya kufika hekaluni na kufukuza wafanya biashara; alitoka nje ya mji wa Bethania akalala huko.


*Maombi hayapotei, hata ikiwa hayajajibiwa kama tunavyotarajia — Ombi la imani halipotei kamwe; lakini kudai kuwa litajibiwa kila wakati kwa njia ileile na kwa jambo lile lile ambalo tumetarajia, ni dhana tu.
--------------------------

Maswali: Mitume walimwambiaje mwenye punda? Unabii wa Zekaria ulisamaje? Kwa nini Yesu ni zaidi ya nabii? Yesu alisema watoto wasipomsifu itakuwaje? Kwa nini Yesu alihuzunika na kulia? Je redio na runinga kueneza injili kunatimizaje unabii wa “mawe yatapiga kelele’.

**SIKU YA 258.**
**(Septemba 14)**

# Mtini kukauka.

**Mathayo 21, Luka 20.**



Asubuhi yake alitoka mapema kabla ya kifungua kinywa, akienda mjini, kisha akaona njaa. Akaona mtini kando ya njia. Akauendea ili aweze kuchuma matunda ale, asione kitu isipokuwa majani yaliyoshamiri kama vile una matunda. Akauambia ule mtini "yasipatikane matunda kwako tangu leo hata milele." Mti ulianza kukauka pale pale. Kesho yake wanafunzi walipopita waliona mti umenyauka toka majani mpaka shinani. Wanafunzi walipoona umenyauka mara walisataajabu wakisema "Jinsi gani mtini umenyauka mara"

Yesu akajibu "Amini, nawaambia mkiwa na imani msipokuwa na shaka mtafanya si hilo la mtini tu, lakini hata mkiuambia mlima ng'oka ukatupwe baharini hilo litatendeka. Na yoyote mtakayoyaomba katika sala mkiamini mtapokea nayo yatakuwa yenu. Nanyi msimamapo kusali sameheni watu, msiweke kinyongo, ili Baba yenu wa mbinguni awasamehe pia makosa yenu, msipowasamehe watu nanyi Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe." Mti ule ulionyauka uliwakilisha dini ya Wayahudi, na hekalu lao lililoonekana zuri nje na makuhani wenye mavazi yenye nakshi nzuri, na nyimbo nzuri za ibada ila Mungu hakuwa kiini. Walikuwa watu wenye maonyesho ya nje kwa mambo ya kidini, ila mioyo na mawazo yao, vilikuwa mbali na Mungu. Yaani walikuwa watu watu wa dini, ila walikuwa wamepotea (religious but lost). Jambo hili limejirudia kwenye jumuiya za waaminio mahali pengi. Mara zingine kizazi cha kwanza cha jumuiya humuamini Mungu kwa unyofu, na kizazi cha pili kwasababu ya imani hii hupata elimu, na kizazi cha tatu hupata mali kwasababu ya elimu, na kwasababu ya imani, ila kizazi cha nne kinaacha imani, yaani kinaasi, na inabidi kianze safari ya kuzaliwa upya tena.

Yesu hakuweka uzito kwenye mwonekano wa nje ikiwa mambo ya ndani ya moyo yalikuwa hayana upendo wa dhati kwa Mungu au watu. Basi zile sherehe na mambo yale ya nje ya ibada yalikuwa utupu. Kwa mfano huu Yesu anatukumbusha maisha ya kuheshimiwa na watu, kwamba wanatuona sisi tu watu wa kiroho tumpendao Mungu, yenyewe peke yake haitoshi kutufikisha mbinguni. Siku itafika watu watatujua, maana watu wataona utupu kwa kuwa hatuzai matunda. Waswahili wanasema uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti. Tunaweza kuonekana tumefanikiwa kwenye masomo yetu, tuna marafiki wengi na tu mashuhuri hapo tulipo; ila tabia zetu haziakisi mafanikio hayo bali kanuni ya kuthamini upendo wa Mungu kwetu na kujali watu. Mtu anayeishi bila kuwa na upendo wa Mungu ndani yake, mwishowe atajikuta hana furaha, na hawezi kuwa na matunda katika jumuiya anayoishi. Hebu tumwombe Mungu ili tuwe na maisha yasiyo ya bandia, maana kwa kuishi maisha ya bandia, tunajidanganya wenyewe na wala si mtu mwingine
Yesu alikuwa amefanya kazi miaka mitatu sasa, na alikuwa amehubiri mahekaluni, nao hawakumkataza, ila walitafuta namna ya kumtega mara nyingi. Walijua maelfu walioponywa, na waliotolewa pepo. Walijua ana uwezo dhidi ya nguvu za asili, maana aliweza kutembea juu ya maji na kutenda miujiza mingi ambayo binadamu wa kawaida asingeweza kuifanya. Hakika hakuna aliyeishi duniani aliyetenda mengi ya ajabu kama Yeye! Akienda hekaluni na wakuu wa makuhani, na wazee wakamwendea na kusema “unatenda haya mambo kwa amri ya nani, naye ni nani aliyekupa amri hii?” Naye Yesu akajibu kwa swali, akisema wakimjibu hilo swali ndipo atawaambia kwamba anatenda haya mambo kwa amri ya nani. “Ubatizo wa Yohana ulitoka wapi? Ulitoka mbinguni au kwa wanadamu?” Watu wakahojiana wao kwa wao, wakisema tukisema, ulitoka mbinguni atatuambia, mbona basi hamkuamini. Na tukisema, ulitoka kwa wanadamu, twaogopa mkutano maana watu wote walimwona Yohana na walimheshimu kama mtumishi wa Mungu hivyo watatupiga mawe. Naye akiwakodolea macho, akawaambia, wala mimi siwaambii ninyi ni kwa mamlaka gani natenda haya.

Akaendelea kwa kutoa mfano wa mtu aliyekuwa na wana wawili akamwambia wa kwanza “mwanangu, leo nenda kafanye kazi katika shamba la mizabibu. Akajibu akasema “Naenda baba” wala asiende. Akamwendea yule wa pili, naye akajibu “sitaki” kwenda, ila baadaye akatubu na kujutia akaenda kuvuna zabibu. “Je kati ya hawa wawili ni yupi alifanya mapenzi ya baba yake,” akauliza Yesu. Wale watu hekaluni wakamwambia yule wa pili. Akawaambia watoza ushuru, makahaba na watu wengine wanaoonekana waovu sasa, wanatangulia mbele yao kuingia ufalme wa Mungu. “Yohana alikuja “kwenu kwa njia ya haki, ninyi msimwamini; Lakini watoza ushuru na makahaba walimwamini nanyi mlipoona, hamkutubu baadaye ili kumwamini.”

Kisa hiki chatufundisha kuwa na kicho na adabu tunapoenda kwenye hekalu, tusiende kujibishana jibishana kule na watu. Mungu anaangalia na kujali sana yale tunayotenda kuliko tunayosema. Hii haina maana kwamba tukipewa kazi na wazazi wetu kwanza tuseme la!, kisha ndiyo twende baadaye. Hapana. Tunapaswa tuseme ndiyo wakati ule wa kwanza tunapotumwa, ila kama tumekosea na kusema la, hiyo itakuwa imemaanisha tumekataa kazi. Ila Roho wa Mungu akizungumza nasi, kwa mawazo au dhamira zetu, tuwe tayari kubadilika. Watoza ushuru na makahaba

walibadilika waliposikia mwito wa Yesu na kuacha njia za uovu za zamani, ila wale waliokuwa wanajua Neno la Mungu kama mafarisayo, waandishi, wazee na makuhani walisema kuwa watu wako tayari kufuata njia Yake, ila ilikuwa ni maneno matupu bila vitendo.

Wanaompenda Mungu Kweli na kumcha, hawapaswi kupenda anasa za dunia au kufanya vile wanayopenda. Ufalme wa mbinguni si ufalme wa upendo tu, bali wa Ukweli, dhati, wema na uaminifu katika tunayotenda na kusema. Kama tunataka tuwe katika ufalme huu lazima twenda kutokana na mipango Yake na sheria Zake. Haijalishi zamani tulikuwa jeuri au tusiotii kiasi gani, twapasa tuungame na kuacha mapito ya zamani, na kugeuka kufanya mapenzi ya Mungu. Je wazazi wakikutuma unasema "sitafanya?", Je Mungu anapokwambia kutii Amri Zake unatii, au unasema "sitatii Amri za Mungu?" Je Mungu anapokwambia utoe moyo wako Kwake, unakataa, kumpa moyo wako? kama ni hivyo kumbuka, kwamba Yesu anakupenda mno, na kama BABA yako, jirudi, na umwambie "nimekosa, nisamehe, nakuja sasa hivi kufanya uliyoniagiza." Anakungojea leo kwenye shamba Lake.

*Malaika hubeba Maombi yetu kwenda Patakatifu pa Mbinguni — Malaika husikia sadaka za sifa na ombi la imani, na hubeba maombi kwa Yeye anayehudumu katika Patakatifu kwa ajili ya watu Wake, na wanasihi haki na sifa Yake kwa niaba yao. Ombi la Kweli hujitegemeza kwa Yeye aliye mkuu na hutupatia ushindi. Akiwa magotini mwake, Mkristo anapata nguvu za kupinga vishawishi.


---------------------------

Maswali: Mwana aliyesema ndiyo asiende anamwakilisha nani? Mwana aliyesema hapana na baadaye akaenda anamwakilisha nani? Mtini ulionyauka unamwakilisha nani?

**SIKU YA 259.**
**(Septemba 15)**

# Mkulima mwenye shamba na watenda kazi waovu.

**Mathayo 21, Luka 20.**



Akatoa mfano wa mtu aliyekuwa na shamba, naye alipanda mizabibu na kushughulikia shamba lake vizuri akazungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo ndani yake, akajenga mnara akapangisha vibarua wa kulima ndani yake akaenda kukaa nchi nyingine. Wakati matunda yalipokuwa karibu akawatuma watumwa wake kwa wale wakulima wavune baadhi ya yale mazao na wamletee. Wale wakulima waliwakamata wale watumwa wake wakawapiga kwa mawe, na kuwafukuza mikono mitupu na wengine hata kuwaua. Akatuma watumwa wengine wengi kuliko wa kwanza wakawatenda maovu, wakiwapiga, kuwaaibisha na kuwajeruhi vichwa, na kuwatupa nje ya ugo vile vile.

Mwishowe akamtuma mwanawe aliyempenda sana kwao akisema "watamheshimu mwanangu." Lakini wale wakulima walipomwona yule mwana, walisemezana wao kwa kwao "huyu ni mrithi, haya na tumwue tutwae urithi wake." Wakamkamata wakamtupa nje ya shamba la zabibu wakamwua. Akauliza "atakapokuja yule bwana wa shamba la zabibu, atawatendeaje wale wakulima." Wakamwambia atawaangamiza vibaya wale wabaya, na lile shamba la mizabibu atawapangisha wakulima wengine, watakaomlipa matunda kwa wakati wake.

Yesu alitoa mfano huu akimaanisha Israeli ndiyo shamba, na Mwenyezi Mungu alishughulikia taifa hili kwa upendo mkubwa, akawalinda akitegemea kwamba matunda yao yatakuwa mazuri. Alivyowatumia manabii Wake kuwaambia habari za ufalme, watu hawa waliwaua manabii hao kwa mawe, na kuwatendea mabaya kama maadui. Mwishowe alimtuma Mwanawe Naye wakamwua, ila hukumu inakuja na hao watu watalipwa uovu wao. Wakati akisimulia walikuwa bado hawajamwua, ila ndiyo walikuwa wanaenda kufanya hivyo. Waliposikia haya walitambua maana yake wakasema "hasha yasitutokee hayo uliyosema."

Yesu akasema "hamkupata kusoma Maandiko, jiwe walilokataa waashi, Hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni; neno hili limetoka kwa BWANA, nalo ni jawabu machoni petu." Akawaambia kwa vile wamekataa jiwe hilo la pembeni ambalo ni Yesu mwenyewe, wao ambao walipata bahati ya kuwa na manabii na Maandiko, basi "ufalme wa Mungu utaondolewa kwao, nao watapewa taifa jingine lenye kuzaa matunda yake." Na hili limetokea sasa kwani Injili au habari za Mwenyezi Mungu zimeenda mataifa mbali mbali na si kwa Wayahudi peke yao. Akawaambia aangukaye juu ya jiwe hilo yaani juu ya Yesu atavunjika vunjika. Kuvunjika huko ni habari njema yaani inaashiria huyo aliyevunjika amejisalimisha kwa Yesu; ila mtu yule ambaye jiwe linamwangukia, litamsaga tikitiki au kuwa unga kabisa.

Wakuu wa mafarisayo na makuhani waliposikia mifano Yake walitambua ananena kuhusu wao, wakaelewa vyema kwamba hawako katika mipango ya Ufalme wa mbinguni bali uovu na kutaka njia zao tu, na si za Mungu. Kutokana na kujisikia hatia walitafuta kumkamata ila waliogopa makutano kwa kuwa walikuwa wanampenda na kumheshimu Yesu kama nabii. Kila mtu alimtambua Yesu kama mponyaji na aliye tayari kumsaidia kila aliyekwenda Kwake. Walimvizia wamnase katika Maneno Yake, wapate kumtia shida na serikali, na kumwua kama ule mfano aliowapa tahadhari nao. Hapo ndiyo waliuliza kama ni halali kulipa kodi, Naye alijibu waipe "serikali cha serikali na Mungu Chake pia."

Watenda kazi wengine katika shamba la BWANA, walifanya kazi kwa uaminifu. Kama mitume, waliwaambia wengi habari za ufalme, na wengine hata leo wanaendelea kufanya kazi kwa uaminifu, wakileta matunda mema, ya upendo, ile Kweli, utu wema, uvumilivu, furaha, na amani. Hata leo wewe una uchaguzi wa kuwa mtendakazi bora kwenye shamba la BWANA, au kuwa miongoni mwa wale wakulima waovu. Kundi gani unalichagua? Yesu alitoa mifano mingi ya kilimo, na mfano kuhusu mti usiozaa. Mti huu ulipewa muda kupaliliwa na kuwekewa mbolea, kwa masharti kuwa usipozaa tena utakatwa, maana unakula chakula na kumwagiliwa maji ila hakuna matunda. Ndiyo hivyo hivyo olivyo katika maisha yetu.
Mungu ametupa muda tubadili uovu wetu, na tusipotaka kubadilika, tutakatwa na kutupiliwa mbali.

*Utalazimika kupambana mieleka na magumu, kubeba mizigo, kutoa ushauri, kupanga mikakati na kuitekeleza, ukimtazama MUNGU kila kwa ajili ya msaada. Omba na fanya kazi, fanya kazi na omba; kama wanafunzi katika shule ya Kristo, jifunzeni kuhusu Yesu.
----------------------

Maswali: Wale wanaoua watenda kazi katika shamba ni wakina nani? Wakulima waliomwua mwana wanafananishwa na nani? Mti usiozaa unawakilisha nini? Jiwe kuu walilokataa waashi ni nini?

**SIKU YA 260.**
**(Septemba 16)**

# Masadukayo, ndoa na ufufuo.

**Luka 20.**



Masadukayo wasioamini ufufuo waliamua nao kumwuliza Yesu kuhusu ufufuo wa wafu. Masadukayo walikuwa watu matajiri, kwenye uongozi wa ukuhani, na walikuwa marafiki kwa kiasi fulani na Warumi. Japo walisikia mafarisayo waliotaka kumtega hawakufanikiwa na swali la ndoa; wao walijipa moyo, kwamba suala lao ni gumu, na watamweza. Hawa hawakuamini ufufuo wala malaika, au vitu vya mbinguni. Hiyo iliwafanya wawe kama wapagani au kafiri, kwani mtu asiyeamini vitu vya mbinguni au ufufuo, hamwamini hata Mungu Mwenyewe, hawa walikuwa ndiyo walikuwa wakiliongoza kanisa enzi zile ila walipenda kufanya maigizo tu. Kama hakuna ufufuo, matofali yanayojenga imani ambayo tunafundishwa kwenye Biblia yameanguka chini. Kama kifo ndiyo mwisho wa mtu na hakuna ufufuo basi Mungu hana mpango na wanadamu baada ya kifo na Yesu asingeweza kufufuka.

Mwokozi aliyebakia kaburini, hana nguvu kushinda mauti na hawezi kuendelea kuwa kuhani wetu. Yesu amefufuka, na hivyo ni ushindi kwetu. Masadukayo waliamini hakuna kiyama na wakasema “Musa alituambia ya kwamba ndugu ya mtu akifa, akamwacha mkewe hana mtoto, ndugu yake amtwae yule mkewe ampatie ndugu yake mzao. Basi kulikuwa na ndugu saba, wa kwanza alioa mke, akafa hana mtoto,

na wa pili akamrithi yule mke kwa kumwoa na naye pia akafa, hana mtoto. Hata wa tatu akamwoa na kumrithi mke huyo, na kadhalika wote saba wakafa, wasiache watoto. Mwisho wake na yule mke naye akafa, basi siku ya ufufuo atakuwa mke wa yupi? Maana aliolewa na wote saba.

Yesu akawaambia wana wa ulimwengu huu huoa na kuolewa, lakini wale wahesabiwao kuwa wamestahili kuupata ulimwengu ule, na kule hufufuka katika wafu, hawaoi wala hawaolewi. Wala hawawezi kufa tena, kwa sababu huwa sawasawa na malaika wa mbinguni, nao ni wana wa Mungu, kwa vile walivyo wana wa ufufuo. Wafu hufufuliwa, maana hata na Musa alionyesha katika sura ya kijiti, hapo alipomtaja BWANA kuwa ni Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, Naye si Mungu wa wafu, bali wa walio hai, kwa kuwa wote huishi Kwake." Watu hawa walifikiri maisha ya duniani yatahamishiwa mbinguni, kwamba yale tunayoona duniani, yatakuwepo mbinguni pia.

Waandishi wengine wa mafarisayo wakakubaliana Naye "Mwalimu umesema sawa" maana wao waliamini ufufuo na Maandiko yote waliyapembua na kuyajua vizuri, bali wasiyafanye na hivyo kuwa wanafiki. Basi watu hawakuthubutu kumwuliza neno baada ya hayo. Kama kifo ndiyo mwisho, imani ya WaIsraeli ya miaka hiyo maelfu haikuwa na maana yoyote, Mungu mwumbaji wa yote, ana nguvu tosha za kufufua. Maisha tuliyo nayo yenye maumivu, kupoteza haki zetu, na mengine machungu, kama yangeishia kwenye kifo tu, basi sisi ni watu wa huzuni sana.

Mungu ni mtoaji wa uzima, na kama aliumba, anaweza kurudisha maisha tena. Kifo ni matokeo ya dhambi, haukuwa mpango wa Mungu kuwa tufe, na wala hatutakizoea kifo, maana ni jambo geni kwa asili ya mwanadamu alivyoumbwa. Ila Yesu arudipo dhambi haitakuwapo tena, milele. Hata hivyo mchakato wa kuachana nayo unaanzia hapa hapa duniani. Kwa neema ya Mungu hatua kwa hatua, tunabadilisha tabia zetu. Wafu waliomkubali Yesu kama Mwokozi wakiwa hai, hao watafufuliwa, kwa uzima wa milele, ndilo tumaini kuu la baraka kwa kila anayemwamini Mungu na kufuata njia Zake za Kweli. Maisha hayo yatakuwa hayana uonevu, magonjwa, maumivu, machozi, au kifo. Je usingependa kwenda mbinguni?

Yesu alifanya muhtasari wa ndoa inavyopasa kuwa katika fundisho hili. Alituelezea kwamba ndoa ni taasisi aliyoiasisi Yeye Mwenyewe na ndoa ni muunganiko kati ya mwanamume na mwanamke. Ndoa ilipaswa kuwa ya kudumu, ila ni dhambi imeharibu mpango wa Mungu ndiyo maana leo wanandoa wanaachana. Ndoa ni ya watu wawili, mume mmoja na mke mmoja na si mwanamke na mwanamke au mwanamume na mwanamume mwingine. Mitara ni kuvunja amri ya saba, na kujiletea maovu mengi kwenye familia zetu. Mume apaswa aache baba na mama na kwenda kuishi na mke wake; mke naye vivyo hivyo. Basi wale waliooa wanapaswa kuzirudia nadhiri za ndoa zao. Watu wa dunia wajue kwamba ndoa ni zawadi takatifu toka kwa Mungu, na wasameheane na kuboresha ndoa zao. Ndoa ni hubiri kubwa, zaidi ya mahubiri ya kibwetani, linalodhihirisha kuwa watu wanampenda Mungu. Wanandoa wanaompenda Mungu wanaweza kufanya mambo makubwa mema, kuliko wanavyokuwa peke yao, Biblia yasema mmoja atafukuza 2000 na wawili

watafukuza 10,000. Wakristo wanaoishi katika ndoa kwa magomvi au mafarakano, wanaipa picha mbaya injili ya Yesu kwa watu wasioamini.

Akawauliza wasemaje watu kwamba Kristo ni mwana wa Daudi? Maana Daudi mwenyewe asema katika kitabu au chuo cha Zaburi 110 "Bwana alimwambia BWANA wangu uketi mkono Wangu wa kuume, Hata niwaweke adui zako kuwa kiti cha kuwekea miguu yako. Basi Daudi amemwita Masihi BWANA, imekuwaje Mwana wake tena?" Wote walikubaliana, kwamba Daudi akivuviwa na Roho wa Mungu akamwita Masihi BWANA. Akawaambia wanafunzi Wake wajilinde na waandishi wa mafarisayo wanaopenda kutembea wamevaa mavazi marefu, na kusalimiwa masokoni, na kuketi mbele katika masinagogi, na viti vya mbele karamuni. Wanakula nyumba za wajane maskini na kuwadhulumu, wakati wao ndiyo wapaswa wawasaidie na kutomaliza kidogo walicho nacho. Pia wana unafiki wa kusali sala ndefu, kutoa sadaka kwa kujitangaza wakipenda maonyesho.

Wengi walisikia siku ile mafundisho yale. Yesu alijua umebakia muda mfupi, na alitaka wasaidiwe na maonyo haya. Alitaka waone unafiki wao na wa viongozi wao, ambao waliweka mizigo mikubwa au vifungo nao wenyewe hawakuwa tayari kuvibeba. Kwa ajili ya unafiki wa viongozi wa makuhani na mafarisayo wengine waliacha imani, na kwa sababu hii Yesu aliamua awaonyeshe watu tabia halisi ya viongozi wao, akafundisha wazi wazi, ili wasiangamie, maana wana wajibu wa kumchagua Mungu kibinafsi, na hawatakwenda mbinguni kwa ajili ya viongozi wao. Waandishi wengine walikuwa upande wa mafarisayo, na hata wazee wengine walikuwa katika makundi haya.
Watu hawa wanyenyekevu, Yesu alitaka wasitangetange, kutoka zizi la Mungu kwa ajili ya uovu wa makuhani.

*Maombi ni njia iliyowekwa na mbingu kwaajili ya mafanikio katika vita na dhambi na ukuaji wa tabia ya Kikristo. Ushawishi wa Bwana unaokuja ili kujibu ombi la imani utatimiza katika roho ya mwombaji yote ambayo anaomba. Kwa ajili ya msamaha wa dhambi, kwaajili ya Roho Mtakatifu, kwaajili sifa na tabia kama ya Kristo, kwa hekima na nguvu ya kufanya kazi Yake, kwa zawadi yoyote ambayo ameahidi, tunaweza kuomba; na ahadi ni, "Mtapokea."
-------------------------

Maswali: Masadukayo waliamini nini? Kwa nini imani ya masadukayo ni dhambi? Mafarisayo walimtega Yesu na swali gani? Yesu aliwajibuje? Kwa nini mafarisayo walikaa viti vya mbele na kusali sala ndefu? Mtu mmoja amesema maombi ya hadhara ni lazima yawe mafupi kwani tutaua roho ya maombi kwa wengine, Wewe unaonaje kuhusu jambo hili?

**SIKU YA 261.**
**(Septemba 17)**

# Ipi ni amri kubwa kupita zingine.

**Mathayo 22.**



Mafarisayo waliposikia Yesu amewafumba vinywa masadukayo, walifanya shauri kwa pamoja mmoja wao mwana sheria akamwuliza kwa kumjaribu akisema, "Mwalimu katika torati ni amri ipi iliyo kuu." Naye akawaambia, Mpende BWANA Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote, hii ndiyo Amri kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako, katika Amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii." Hatuwezi kugusa mbingu bila kugusa binadamu. Tunaposogea karibu na Mungu ndivyo tunavyosogea pia kwa binadamu wenzetu. Hatuwezi kuwa watawa na kuepuka watu.

Wote inatubidi kutosahau kumwomba Mungu. Maombi ya faragha ndiyo sira ya nguvu na ushindi. Tuyafahamu anayotuambia na kuyatimiza kwa vitendo. Mwanamke mwingine alipomwona Yesu aliona wivu na kusema "Heri tumbo lililokuzaa na matiti uliyonyonya." Lakini Yesu alisema ni afadhali na ni heri wale walisikialo Neno la Mungu na kulishika. Inatupasa daima kuyafuatilia yale mambo mema na kuyatenda maana tunajaribiwa kufanya uovu mara nyingi. Kwa kuwa kuna siku ambayo vyote vinavyofanyika kwenye giza Mungu atavifunua na kuviweka hadharani.

Mtu mwingine alikuja kwa Yesu ili aamuliwe kesi yake kwa kuwa baba yao alikufa na nduguye alikatalia urithi. Yesu akamwuliza ni nani amekwambia Mimi niwe mhukumu wa mambo haya? Akasema maisha ya mtu hayategemei vile alivyo navyo. Hapo akatoa mfano wa mtu aliyepata mavuno mengi hadi ghala zake zikajaa na kuanza kujidai, "wacha nibomoe ghala zangu ili nijenge ghala kubwa" asijue usiku atakufa na kuacha yale yote wakati hajafanya uamuzi wa kumfuata Yesu. Wakati mwingine mtu hujitumainia na kupanga mipango na malengo yake bila kumshirikisha Mungu, wala bila kujua kitakachozaliwa na siku moja. Kulimbikiza mali bila kujua kwamba maisha yake nayo ni upepo, bila hata kuzingatia kutoa huduma kwa jamii wala kusaidia kazi ya Injili huko nako ni kukosa lengo, kwani siku moja mali yote ya dunia, itakuwa majivu.

Kuna watu wawili pia walijenga nyumba mmoja kwenye msingi wenye michanga tupu na mwingine kwenye msingi wa mawe, upepo na tufani vilipokuja yule aliyejenga kwenye mchanga ilianguka, bali yule mwenye nyumba iliyosimama kwenye jiwe, ilisitikira wakati viasili vya tufani na vingine vilipokuja. Mtu anayemwamini Mungu, anafananishwa na mtu aliyejenga nyumba yake juu ya Mwamba. Mwamba katika Maandiko ni Yesu Kristo. Leo tunashauriwa tujenge juu ya Mwamba huu, tumpende Yeye kwa mioyo yetu yote, akili zetu zote, nguvu zetu zote, na kwa roho zetu zote na jirani kama nafsi zetu. Maneno ya Yesu hayawezi kuelezeka kisayansi, au kwa maarifa na falsafa za binadamu bali kwa uwezo wa Roho wa Mungu. Elimu zozote za dunia ni pungufu mno kuelewa yanayohusu wokovu wetu, bali Roho Mtakatifu Ndiye atusaidiaye kuelewa. Hivyo tusisome Maandiko bila kumwomba Mungu atupe nuru ya kutuangazia kuyaelewa.

Tabia zetu daima ziko kwenye ujenzi; kama tabia hizi tunazijenga kwenye Mwamba yaani juu ya Yesu, basi shida na masumbufu ya maisha haya hazitatuchukulia mawazo yetu yote hata tuingie kwenye mitego ya Shetani. Maisha yetu lazima yajengwe kwenye mafundisho thabiti ya Yesu. Yeye Ndiye Mwamba usiotingishika. Ndiye kimbilio letu na msingi imara. Tusiangalie kama ni wengi wanaunga mkono ule upande tuliochagua, bali tujiulize ikiwa jambo tunaloliamini linaafikiana na Maandiko ya Mungu au limejikita kwenye Mwamba? Watoto walipoenda kumsikiliza Yesu alichosema walielewa vizuri na wakachukua alivyosema bila kuona kwamba wengi wanafuata au hawafuati.

Mtoto anayempenda Yesu na kutaka kufuata Maagizo Yake, aweza kuwa mtenda kazi wa Mungu bora kuliko mtu mzima. Kwa vile anajua kwamba ana upungufu, anakuwa na kiu ya kumtafuta Mungu na kumtegemea kuliko kawaida. Mtoto wa namna hii atafanikiwa kujenga jengo imara kuliko watu wazima walio na maarifa mengi, na talanta nyingi, kwa sababu anamfuata Mungu na kumtegemea katika mipango yake yote. Tukijitoa kikamilifu, tutajua kwamba tunajenga kwenye mwamba au mchanga. Tutajua kama Mafundisho tunayofuata ni ya Kweli au ni mapokeo ya watu.

*Maombi yetu yanapaswa kuwa ya bidii, ya dhati na ya kudumu kama ilivyokuwa ombi la yule rafiki masikini aliyekwenda kuomba mikate usiku wa manane. Kwa kadiri tunavyoomba kwa bidii na uthabiti, ndivyo muungano wetu wa kiroho na

Kristo utakavyokuwa wa karibu zaidi. Tutapokea baraka zilizoongezeka kwa sababu tumeongezeka kiiimani.


---------------------------

Maswali: Ipi ni amri kubwa kupita zote? Yesu alisema ni nani ana heri hata kupita mama Yake mzazi? Kujenga juu ya Mwamba ina maana gani? Utajuaje kama unajenga juu ya mchanga? Yesu alimjibuje mtu aliyetaka afanye kesi ya ndugu aliyempunja urithi?

**SIKU 262**
**(Septemba 18)**

# Ole wa Mafarisayo.

**Mathayo 23.**



Yesu aliwapenda watu wa matabaka yote, na akatafuta mwanya azungumze nao ili wapate wokovu. Aliwapenda mno, ndiyo maana hakukaa kimya akiwaachia wapotee. Aliwaambia waliyopaswa kusikia. Nasi pia tusitafute kuwa na amani kiasi kwamba ile amani itufungamanishe na kutusahaulisha Kanuni za Ukweli. Hakuna ambaye atakayefuata Kanuni za Kweli ya mbinguni na haki, bila ya kuwa na maadui. Yesu alisema wasiogope yule anayeua mwili, bali anayeua roho. Yesu hakuwapa Mafundisho Makuu ya imani tu, bali pia aliwaambia kuhusu upendo wa Mungu. Mafarisayo wengi walisema Ukweli bila upendo. Nia zao zilikuwa na uchoyo, ujeuri au hila fulani.

Walikazania matendo ya nje ya kuonekana, wakisahau mawazo, nia na moyo vinavyopaswa kubadilika kwanza. Mafarisayo waliorodhesha sheria za Musa mpaka zikafikia 613. Kisha wakachukua kila moja ya hizi na kuongeza zao wakisema zitasaidia kutunza hizo 613. Ndipo walipojipatia maelfu ya amri, ambazo zilikuwa mzigo au kongwa kwa watu. Yesu akawaambia makutano na wanafunzi Wake, akisema, waandishi wa mafarisayo wameketi kitini mwa Musa kama viongozi wa na wanayajua Mafundisho yote, basi yoyote watakayowaambia myashike na kuyatenda, lakini kwa mifano ya matendo yao msiige, maana hunena mambo sawa ya Sheria na Kanuni za Mungu ila hawatendi. Ila wanawatwika watu mizigo mizito mabegani wasitake wenyewe kuigusa kwa kidole chao.

Watu wa namna hii huitwa wanafiki, maana matendo yao yote huyatenda ili kutazamwa na watu, kwa kuwa hujivika vikasha vya mafungu ya Biblia vipajini mwa nyuso. Hupenda kuketi mbele ya masinagogi na kusalimiwa masokoni na kuitwa na watu, Rabi. Bali nyinyi muwe tofauti msiitwe na watu Rabi maana mwalimu wenu ni mmoja nanyi ni ndugu. Wala msimwite mtu baba duniani, maana Baba yenu ni mmoja, aliye mbinguni. Wala msiitwe viongozi kwa kuwa kiongozi wenu ni mmoja Naye ni Kristo. Na aliye mkubwa ndiye mtumishi au msaidizi kwa wengine, na yeyote ajikwezwaye atadhiliwa naye atakayejidhili atakwezwa. Yesu aliendelea

kusema anawahurumia mafarisayo.

Ole wenu waandishi na mafarisayo wanafiki, mnawafungia watu kuingia mbinguni ninyi wenyewe pia hamwingii na wanaotaka kuingia hamwachi waingie. Ole wenu waandishi na mafarisayo, kwa kuwa mnakula nyumba za wajane masikini na kwa unafiki mnasali sala ndefu, kwahiyo mmejipa hukumu kubwa zaidi. Ole wenu waandishi na mafarisayo kwa kuwa mnazunguka baharini na nchi kavu kwa bidii kupata mtu mmoja kuwa mwongofu na mkisha mpata, mnamfanya kuwa mwana wa Jehanamu mara mbili zaidi kuliko nyinyi wenyewe. Ole wenu viongozi vipofu, ninyi msemao, Mtu atakayeapa kwa hekalu, si kitu; bali mtu atakayeapa kwa dhahabu ya hekalu, amejifunga. Wapumbavu nyinyi na vipofu, maana dhahabu si muhimu bali hekalu ndiyo inafanya dhahabu kuwa na thamani. Mtu anayeapa kwa madhabahu ndiyo shida na si anayeapa kwa sadaka iliyo juu ya madhabahu. Msiape hata kwa mbingu pia ni kiti cha enzi cha Mungu.

Ole waandishi na mafarasyo wanafiki mnalipa zaka za mnanaa, giligilani, binzari na viungo vya mboga ndogo ndogo wakati mmeacha mambo Makuu ya Sheria yaani adili na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya. Mnachuja mbu na kumeza ngamia. Ole wenu waandishi wa mafarisayo wanafiki kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na ndani mmejaa unyanganyi na kutokuwa na kiasi. Ewe farisayo, kipofu safisha kwanza ndani ya kikombe ili nje yake nayo ipate kuwa safi.

Wengi walijua tabia ya mafarisayo wakatingisha vichwa vyao wakiafikiana na Yesu. Mafarisayo walitaka kujiweka kwenye nafasi za juu ila hawakuwa na upendo. Walijua unafiki wao ila hawakujua jinsi ya kuepuka 'siasa za kanisa'. Yesu alitaka watu wajue mwonekano wa nje si wa muhimu sana kama moyo wa mtu ulivyo. Bongo za mafarisayo zililijaa elimu ya Maandiko Matakatifu, ila mioyo na nia zao zilijaa uozo wa dhambi. Yesu hakutaka kuwakashifu au kuwazomea viongozi hawa wa dini, au kuwafanya wapandwe na hasira, bali alitaka kuwasaidia kwa mara ya mwisho. Alitaka kutafuta na kucheua mambo ili watubu, na kuwa na mioyo ya dhati ya kumpenda Mungu na watu, si kujipenda wenyewe, kula rushwa na hila zingine. Maandishi hayatujulishi sauti au mwonekano wa uso wa Yesu, ila twajua Mungu anatafuta wokovu wetu kwanza hata kabla ya sisi. Ni Yeye Ndiye anayetuvuta. Alizungumza wazi wazi siku hii ili kila mtu aelewe wazi wazi na kujirudi. Mbali na kufanya dhambi na kuanguka, walikuwa wameangusha wengi, waliochoka na unafiki wao, hata kuacha imani. Je una viongozi au wazazi ambao hawafuati mafundisho yale wanayosema? Yesu aliona shida hiyo, akazungumzia, na kila mtu akaelewa. Alitaka kuhakikisha kwamba hawapotei, na kutangatanga kama kondoo bila mchungaji kwa vile wachungaji walikuwa wanaonesha mfano mbaya.

Jambo moja muhimu ni kwamba karibu wanadamu wote hata Wakristo na viongozi wana kawaida ya kuigiza tabia ya mafarisayo. Mtu hahitaji kuwa injinia wa Roketi, au talanta nyingi kuwa mnafiki, hasa kama ni mtu mzima. Ni watoto, walevi na wenye maradhi ya akili tu, ndiyo hawawezi kuiga tabia za mafarisayo, wao husema ile Kweli yote na kuishi maisha halisi, yaani yasiyo ya unafiki. Ni kweli mafarisayo walikuwa Wayahudi, bali walikuwa na silika yetu binadamu wote, hivyo kila mtu mkristo au muumini anapaswa kusoma Mathayo 23 daima na kuomba maombi ya

Zaburi 139 "unijaribu BWANA uyajue mawazo yangu, Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, Ukaniongoze katika njia ya milele." Tujiulize mara nyingi je tunaishi kulingana na yale tunayosoma? Je tunapenda watu watuone na dini yetu na vyeo vyetu, na kusahau huduma kwa Mungu ni kujitoa mhanga?

Tendo moja bovu au dhambi fulani tunayoirudia tena na tena, tusitake kuiacha, inafanya tabia yetu kuwa dhaifu, na kuwapoteza wengine. Mafarisayo walikuwa hawapo tayari kubadilika, wakarudia unafiki, na uovu, mpaka tabia ikaota sugu au kuota mizizi. Hata sisi tuache tabia zetu za ubinafsi na kufuata mfano wa Yesu, kwa kubeba msalaba.

*Fungu letu ni kuomba na kisha kuamini. kesheni mkiomba. Kesha, na ushirikiane na MUNGU anayesikia maombi. Kumbuka kwamba "sisi ni watenda kazi pamoja na MUNGU." 1 Wakorintho 3: 9. Sema na kutenda kulingana na maombi yako. Na hilo litafanya tofauti kubwa kwako pale jaribu litakapokujia ili kuhakikisha kuwa Imani yako ni ya Kweli, au kuonyesha kwamba maombi yako ni mfano tu.
-------------------------------

Maswali: Kwa nini si hekima kufanya wengine kwenda Jehanamu? Kusafisha kikombe ndani kwanza ina maana gani? Kwa nini Yesu alikaripia uongozi wa kanisa mbele ya umati? Kuna mambo gani leo unayafanya kama mafarisayo?

**SIKU YA 263.**
**(Septemba 19)**

# Mafarisayo.

**Mathayo 23.**

Yesu aliendelea kutoa tahadhari akisema 'Nawahurumia Mafarisayo' au Ole wao waaandishi na mafarisayo ambao walijionyesha kwa matendo ya nje na kukaa kwenye viti vya mbele kwenye masinagogi na karamu, kuwapunja wajane, kunyenga chakula cha masikini, na kuwatwisha mizigo watu bila wao kugusa hata kwa kidole kimoja. Walikuwa wakipenda kuitwa majina makubwa makubwa na wafuasi, kama vile baba, Mwalimu, na mengine ambayo ni Mungu tu anapaswa kuitwa. Walipenda watu wawanyenyekee na kuwaabudu.

Yesu alipoishi duniani kulikuwa na Sheria za aina nne: za Musa, za marabi, za Warumi na zile Amri Kumi za Mungu. Mafarisayo walihesabu sheria 613 za Musa na kuongeza zao katika kila moja, zikafanya kuwe na maelfu ya sheria. Waandishi walipata nafasi ya kunakili Maandiko kwa vile kulikuwa hakuna mashine za chapa, na kusaidia kuwafundisha watu wamjue Mungu. Walikuwa kwenye kiti cha uongozi kama Musa ila wasifanye wajibu wao kwa watu au kwa Mungu. Walipewa muda kujisahihisha lakini hawakusaidika. Hiyo ndiyo shida ya unafiki; kupenda kudanganya watu, hatimaye kuamini ule uongo na kujidanganya mwenyewe.

Yesu akasema, Ole wenu waandishi wa mafarisayo wanafiki, kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa na kuonekana maridadi, bali ndani yake yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote. Vivyo hivyo ninyi nanyi kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenye haki, bali ndani mmejaa unafiki na maasi. Watu hawa walitumia pesa nyingi kujengea wafu minara, badala ya kusaidia wagonjwa na wenye mahitaji, kabla hawajafa. Walifanyia watu vile wasivyohitaji, na kuwanyima watu mema waliyohitaji.

Ole wenu waandishi wa mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnajengea makaburi ya manabii mapambo na maua, mkisema kwamba "tungalikuwako zamani za baba zetu, hatungalishirikiana nao katika kuua hawa manabii. Hivi mwajishuhudia wenyewe kwamba watu wanaosema ni wa Mungu waweza kuwafanyia ukatili manabii na hata kuwaua. Kama hili lilitokea enzi zile, basi hata sasa linatokea kwenu. Mnapanga kuniua saa hii hii, mkijaza kibaba cha kipimo cha baba zenu au mkifanya matendo sawasawa na wao. Ninyi ni kama nyoka na wana wa nyoka maana mna sumu na uovu, mtakimbiaje hukumu ya Jehanamu? Kifo Changu hakitakuwa mwisho wa chuki na uovu wenu maana natuma manabii na wenye hekima walimu na waandishi na wengine wao ndio nitawaua na kuwasulubisha. Mtawapiga katika masinagogi yenu, na kuwafukuza mji kwa mji,

Akasema wametesa manabii toka kuanzia misingi ya ulimwengu wakiua watu wenye haki, ambao ni watumishi wa Mungu wanaotaka kushika Maagizo Yake, tokea Habili mpaka Zakaria aliyeuwawa kwenye madhabahu ya Patakatifu pa

hekalu na mfalme Yosia. Waliuondoa ufunguo wa maarifa na wenyewe hawakuingia na walioingia waliwazuia. Waliposikia haya waandishi na mafarisayo walianza kumsonga vibaya na kumchokoza kwa maswali mengi. Kutoka pale walimvizia ili wapate Neno litokalo kinywani Kwake ili wapate sababu ya kumshitaki au kumwua. Yesu akasema kwa huzuni "Eh Yerusalemu, Yerusalemu uwauaye manabii na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Laiti ungelijua yapasayo amani kwako! Ni mara ngapi nimetaka kukusanya kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka! Angalieni nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa wa kutokuwa na uwepo wa Roho wa Mungu, kwa ajili ya kiburi chenu na kutosikia." Akaishia kwa kusema "hamtaniona kamwe tangu sasa hata mtakaposema, Amebarikiwa Yeye ajaye kwa Jina la BWANA." Basi Yesu alitoka hekaluni.

Yesu alitaka wote waelewe kwamba anawajali mno aliposema ni mara ngapi amewakusanya kama mama kuku akusanyavyo vifaranga vyake ili wawe katika usalama na mwewe au tufani ipitapo, ila hawakutaka kusaidiwa. Hakutaka kuwaaibisha, ila walikuwa wamezidi kipimo cha dhambi na vituko, akatoa nafasi ya mwisho kuwaonya tena. Hata nasi leo anatuonya tuwe makini. Je, tunalisoma Neno Lake? Je tunalitenda? Watoto kwa wakubwa wapi tumekosea tujirudi, ili tusiwe waigizaji. Yesu alikuwa anazungumza na wacha Mungu, washiriki kanisani na wala si viongozi wa siasa au nchi au wapagani wa Sidoni.

Mtu mmoja alisema kwamba waumini wengi huishi kama waigizaji, na kusimulia kisa cha Yesu cha msalaba kama wanaigiza ila moyo wao haumo humo. Bali wacheza filamu wao huigiza kama wanaishi kihalisi, japo wanaigiza. Yabidi tumtafute Yesu na kumjua, ili tukiwaambia watu wengine habari Zake, tusionekane kama waigizaji, bali watu tunaosema mambo halisi yatakayotokea. Leo wote walio kanisani ni wakati wa kukaa chonjo. Tamaa ya macho, tamaa ya mwili, na kiburi cha maisha haya ni kinga zaidi ya siku zile za Yesu. Hatuwezi kupona tusiponyenyekea Kwake na kujisalimisha. Makuhani na waandishi walijali mali, na sifa kutoka kwa watu na pia walionea watu.

Haya yameandikwa kwa ajili yetu, na si kwa ajili yao. Wao mafarisayo waliambiwa kwa mdomo ili yawasaidie, maana tunayoyasoma leo yalikuwa hayajaandikwa bado. Inawabidi waumini wakeshe na kuomba ili kusiwe na dini ya uongo, hasa makanisani. Mtu anaweza kupotea akiwa kanisani kama mafarisayo. Tukiwachosha watu na sheria hizi au zile, twaweza kuwakimbiza watoke nje ya kanisa. Sheria au Maandiko ni muhimu, hata Yesu hakuvunja Sheria, na ilibidi afe ili Maandiko au Sheria itimie. Yesu hakuvunja hata Amri moja ya Mungu, hakuwa mvunja Sheria, alizitunza sheria, ila hakuwa mnafiki.

Mtoto wangu wa miaka saba alisema siku moja nilipowachelewesha kwenda kanisani "mama wewe ni mnafiki, mbona unasema tuwahi kanisani na wewe mwenyewe unachelewa?" Aliwahi kwenye gari akaningoja pale ili twende, maili 25 tulipokuwa tukisali. Je kuna shida hii nyumbani mwenu? unajitahidi kufanya mambo mema ila wazazi wako wanakurudisha nyuma nao ndiyo walikuleta kwenye imani? Utasema kwamba kama wengine ni wanafiki una sababu nawe ya kuwa mtu mbaya au

mnafiki! La! hasha, mtu mwingine akiwa mnafiki, ndiyo wakati wewe wapaswa kuchukua jukumu la kuonyesha picha au mfano mzuri ili wengine waufuate, na kuvunja mnyororo wa uovu na unafiki. Sema "BWANA naishi na wanafiki, na wana mifano mibaya kwangu. Ila naomba unisaidie kuwajibika kwa ajili yangu mwenyewe, na kwa ajili ya wengine na mbele Zako Mungu; kuonyesha mfano bora, wakati dunia ina watu walioojaa unafiki, nisaidie mimi, ili mtu atayeniangalia, aweze kupata mfano bora na achague uzima, badala ya unafiki."

Napenda kusema machache ya unafiki, kwa vile ni rahisi sana kuwa mnafiki kama mafarisayo. Watoto wadogo wote, siyo wanafiki; ni wasema Kweli na wanapenda kuwa katika uhalisia. Ndiyo maana Maandiko yanasema ufalme wa Mungu ni wa watoto wadogo. Jinsi mtoto anavyozidi kuwa mkubwa ndivyo anaingia dhambi ya unafiki. Kila mtu mzima amefanya dhambi hii. Safari yetu ya maisha ina mistari mitatu au njia tatu sambamba. Mstari wa katikati, ni injili na upendo wa Yesu, ni ile njia ya uzima ambayo Mungu ataka tuifuate. Kushoto kuna unafiki, ni kujua Biblia ila kuishi maisha tofauti, kuwaambia watu wengine wanafanya maovu, ila sirini, mtu anafanya maovu hayo. Kuipita njia ya kushoto ni kuwa mtu wa dunia, wa kuishi kwa anasa, na kutomwamini Mungu.

Kila binadamu anateleza na kukuta anaegemea kulia kwenye dunia au kushoto kwenye unafiki. Ni rahisi sana kuwa shabiki wa upande mmoja aidha kupitiliza kila kitu kiwe ruksa, au kuwa mhafidhina Ni Yesu tu, Ndiye ambaye tukijisalimisha Kwake, na tukimkiri na kumwomba atatupa neema Yake, atatusaidia kuelekea kwenye msimamo sawa na si kushoto au kulia, basi tutamtazama Yesu Kalvari, na kupewa kuishi. Basi wazazi wakiwa karibu na Mungu kwa mahusiano, inafanya Roho wa Mungu kusaidia tabia za watoto wasiwe wanafiki. Yesu anajua mzigo ambao wazazi wanao, atawasaidia kuwatunza watoto na wazazi wasiwe wanafiki au watu wa dunia.

*Maombi ya dhati na bidii yana manufaa mno — Sala ile inayotoka katika moyo wenye bidii, na mnyofu, na unaoamini ndiyo itakuwa na matokeo mema, maombi yenye bidii ambayo yatakuwa na matokeo makubwa na mema mno. MUNGU huwa hajibu maombi yetu kila wakati kama tunavyotarajia, kwani hatuwezi kuombea kile ambacho kingekuwa bora zaidi kwetu; lakini kwa upendo na hekima Yake isiyo na kikomo atatupatia vile vitu ambavyo hakika tunavihitaji.
-------------------------------

Maswali: Makaburi yalirembeshwa bali yalikuwa na nini ndani yake? Mfano wa kuku na vifaranga unatuonyesha nini? Kwa nini Wayahudi waliua manabii? Je una tabia gani ya unafiki ambayo inabidi uachane nayo? Je nini Leo unachofanya au wanachofanya kanisani kinachofanana na mafarisayo?

**SIKU YA 264.**
**(Septemba 20)**

# Yesu anarudi upesi, Je dalili za kuja Kwake ni zipi?

**Mathayo 24.**



Je, unajua dunia hii ipo katika ukingo wa historia yake. Karibu kila unabii umetimizwa. Unabii uliobaki ni ule utakaofanyika kwa muda mfupi. Wajua jinsi mtu anavyoweza kujitayarisha ili Yesu akija aende Naye mbinguni? Yesu alipotoka Hekaluni, wanafunzi Wake walimjia na kumwonyesha yale majengo ya hekalu. Wayahudi wengi walijivunia hekalu lao, lililochukua miaka 46 kujengwa na kwa hakika, kiini cha uchumi wa nchi hiyo, kilihusu mambo ya hekalu, kwa ajili ya zile kafara. Wayahudi wakasahau zile kafara ni mfano tu au kivuli, ila kafara ya Kweli ni Yesu Mwenyewe, Mwana-Kondoo wa Mungu anayeenda kuchinjwa kwa ajili ya dhambi za watu. Damu za kondoo hazikusaidia kuokolewa, zilikuwa kama picha au kielelezo.

Yesu aliwaambia haya majengo yote "halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomolewa." Hata alipokuwa ameketi katika mlima wa mizeituni wanafunzi Wake walimjia wakisema "tuambie mambo hayo yote yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja Kwako, na ya mwisho wa dunia? Naye akawajibu jibu ambalo ni letu sote. Yesu akijua wanafunzi wana hofu na kuchanganyikiwa na mambo yote, aliwaeleza, udanganyifu utakaotokea kama dalili za kuja Kwake; bali wao waishi daima kwa matumaini wakitazamia ujio wa Yesu. Wengi watatokea kudanganya watu, manabii wa uongo wakisema "mimi ni Kristo" na watawadanganya wengi, hata wale ambao wanaonekana ni imara, kama wasipochukua tahadhari ya kumtegemea Mungu kikamilifu.

Hivyo hata leo sisi sote tuchukue tahadhari hii kama dalili ya kwanza ya kuja kwa Yesu, au mwisho wa dunia. Watu wengi wameshatokezea kusema wao ni manabii. Rafiki yangu mmishonari Kongo aliniambia kwamba walifika kijiji fulani kule, na walipoingia nyumba moja, kuna mtu alisema Yeye ni Mungu BABA na kijana wake ni Mungu Mwana. Alipata wafuasi maelfu pale na wakamwabudu. Ila siku moja aliugua kuharisha vibaya, na akafa, akiwa na miaka arobaini hivi. Kijana wake kwa woga naye aliacha kukufuru kwa kujiita Mungu Mwana. Siku hizi hata wanawake wametokezea kusema wao ni Mungu. Hii haikuwahi kutokea huko zamani. Wanawake wengi hii haikuwa dhambi yao, waliweza kusema wao ni manabii (wa uongo), au wachungaji lakini hawakusema wao ni Mungu kama dini za mashariki na ulaya zenye miungu ya kike.

Dalili zingine ni vita na tetesi za vita. Taifa au ufalme utaondoka kupigana na taifa, na kutakuwa na njaa, na matetemeko kila mahali na nyota za mbinguni zitaanguka. Miaka 200 iliyopita kulikuwa na matetemeko machache ila sasa matetemeko yanazidi kuongezeka na hata kufikia idadi ya mamia kila mwaka. Jinsi siku zinavyokuwa karibu na ujio wa Yesu, ndivyo mioto, mafuriko, uharamia, mauaji, na majanga mengine yanavyozidi kuongezeka duniani. Haya yote ndiyo mwanzo wa utungu na dalili za kuja kwa ufalme wa Mungu. Ni kama mama apatavyo uchungu kabla ya kuzaa.

Wakati huo watu watawasaliti ninyi mpate dhiki na kuwaua. Wengine watakaowasaliti mtashangaa maana mlikuwa mnafikiri ni washiriki wenzenu na kumbe ni makapi au magugu. Mtakuwa watu wa kuchukiwa na mataifa yote kwa ajili ya Jina Langu. Ndipo wengi hata washiriki wa kanisa walioonekana imara watajikwaa, wakisalitiana na kuchukiana. Wahubiri na manabii wa uongo watatokea kila mahali wakilaghai watu. Kwa sababu ya kuongezeka uovu, upendo wa watu utapungua, maana watu hawatajua maana ya upendo wa Kweli, kwa jinsi uovu ulivyoshamiri kwenye maisha yao. Wengi watakuwa na upendo wa mdomoni, tu bali watakuwa na nia mbaya kwa watu.

Yaonekana dalili zote ni mbaya isipokuwa ile ya "Habari njema za ufalme zitahuburiwa katika ulimwengu wote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote, hapo ndipo ule mwisho utakapokuja." Leo, watu wanatafuta mambo ya kiroho usiku na mchana. Mwaka wa 2013 vitabu vya kiroho viliuzika kupita vitabu vingine vyote. Hii inaonesha watu wanatafuta mambo ya kiroho kwa bidii sasa. Kitabu kilichokuwa cha kwanza kwa kununuliwa ilikuwa Biblia, na cha pili kilikuwa Kitabu cha Kurani, na cha tatu kilikuwa kitabu cha Mao chekundu (Red book of China). Vyote hivi vinahusiana na mambo ya kiroho.

Yesu akasema mtakapoona kile Nabii alichosema kama "chukizo la uharibifu" likiijia Yerusalemu na kusimama katika Patakatifu, basi asomaye na afahamu kuwa nyakati mbaya zimewadia. Unabii huu ulikuwa na maana mbili; maanguko ya Yerusalemu mwaka 70BK, na kisha maanguko ya dunia na kuja mara ya pili kwa Yesu katika nyakati za siku za mwisho. Kwa vile sisi ndiyo tunaishi siku za mwisho, hebu tusome mambo haya, tutafakari na kuyatenda. Akawaambia yakitokea hayo wasishuke kutoka darini walikokuwa wanashinda mchana kutwa kwa kutokana na

joto, na kuja kuvichukua vitu vya nyumbani mwao kama nguo na kadhalika. Na aliye shambani asije nyumbani kufunga mizigo yake ndipo aende, maana hatakuwa na muda na itakuwa rahisi yeye kuonekana na kukamatwa. Itakuwa shida kubwa kwa wale walio waja wazito, na wanaonyonyesha kukimbia wakati huu wa dharura. Akasema tuombe ili siku hizo za kukimbia milimani zisiwe siku za baridi ya barafu au siku ya Sabato, maana haitapendeza pilika hizo za kukimbia ziwe siku takatifu ya ibada au majira ya barafu na baridi kali. Na kama Mungu hataingilia kati au kufupiza mateso hayo, hakuna atayeokoka. Yesu ametuambia kwamba kabla hajaja habari njema itahubiriwa hadi miisho ya dunia. Leo tuna vyombo vya habari ambavyo havikuwepo zamani hizo, vinavyotumika kupeleka habari njema kama vile: vipaza sauti, Projekta, mashine za kuchapa magazeti na vitabu. Wakati huu tunashuhudia kutafsiriwa kwa Maandiko kwa zaidi ya lugha 2,000, na uvumbuzi wa redio, runinga, Kompyuta, simu na kadhalika. Yesu hakusema kila atakayesikia ataamua kumkubali Mungu. La! bali alisema mtu huyo atakuwa ameshuhudiwa, na kuamua mwenyewe ikiwa anataka kumfuata Yesu au la; ili asimlaumu mtu.

Yesu hatakuja kwa kujificha, bali kutokea Kwake kutakuwa kama kuonekana kwa umeme na radi kutoka mawinguni. “Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Kila mtu atasikia na kumwona, kila lugha taifa na jamaa wawe Waaustralia, Wakenya, Waganda, Wanyarwanda, Wachina, Wahindi, Wamarekani, Waperu, Wakurdi, Waswisi, Watanzania au Wafilipino. Kitabu cha Wathesaloniki kinatwambia, litakuwa si jambo la siri, kwani parapanda zenye sauti kubwa na kila jicho duniani litamwona wakati huo, yaani litamwona akija. Na wale waliojiweka tayari watachukuliwa kwenda mbinguni, Mpinga Kristo ataangamizwa kabla ya safari ya kwenda mbinguni! Hakuna nafasi ya pili ya kuokolewa, kwamba wengine wanatwaliwa na wengine kuachwa, eti wajitayarishe na kuja kuchukuliwa tena! Adui ataka kutudanganya kwamba tutakuwa na nafasi ya pili ya kuokolewa katika nadharia ya unyakuo, hii haiendani na Biblia. Na hilo ni tosha kuondoa nadharia ya kunyakuliwa ambayo haipo kwenye Maandiko na miaka ya hivi karibuni kupitia mafundisho ya Schofield Biblia na Tim LaHaye. Hata kiziwi atawasikia malaika na sauti ya parapanda. Mbingu zitakunjwa kama ukurasa, na watu mashujaa na mashuhuri, wafalme na matajiri, na wale wasiomtafuta wakati huu wa amani, watajificha kwenye mapango na kuomba milima iwaangukie.

*Maombi ya bidii na ya daima au kudumu ni ya lazima — Ikiwa Mwokozi wa wanadamu, Mwana wa MUNGU Mwenyewe, alihisi hitaji la maombi, Je, ni muhimu kwa kiasi gani zaidi basi kwa sisi wanadamu tulio dhaifu na wenye dhambi tunatakiwa kuhisi umuhimu wa maombi ya bidii, kila wakati?

------------------------------

Maswali: Kwa nini Yesu anataka tujue dalili ya siku za mwisho? Dalili gani zitatuonyesha tupo siku za mwishoni? Yesu alijibuje mitume walipojivunia hekalu? Kwa nini si hekima kujivunia kazi za mikono ya binadamu?

**SIKU YA 265.**
**(Septemba 21)**

# Dalili za siku za mwisho.

***Mathayo 24***



Kwa ajili ya wateule wanaomlilia Mungu usiku na mchana Mungu atafupisha siku hizo za taabu, ili aokoe wale wanaomtumaini na kumtegemea Yeye. Mtu akisema siku hizi Kristo Yupo hapa au pale, msimsikilize kabisa, maana watatokea wakristo na manabii wa uongo, na wengine watasema mimi ni Kristo, na kumbe ni uongo, na Ibilisi atawapa waongo hawa nguvu za kutenda miujiza ya aina fulani, wapate kupoteza watu yamkini hata wateule. Cha muhimu ni kwamba Kristo atakapokuja mara ya pili hatakanyaga ardhi hii. Atakuwa angani na watu ndiyo watanyakuliwa kumlaki mawinguni. Hivyo ukisikia mtu anasema ni Kristo yulee kwenye duka au mahali fulani, na bado anakanyaga dunia, ujue hapo kuna walakini; japo atende ishara kubwa na maajabu. Yesu alikwisha kutuonya kwamba wakisema "Yupo jangwani, yupo nyumbani" tusisadiki. Kama vile umeme kabla ya radi utokavyo mashariki ukaonekana magharibi ndivyo kuja kwa Yesu kutakuwa. Kutakuwa na mengi yatakayotokea ila wale waliojisalimisha kwa BWANA na kumtumaini watajua mwisho u karibu sana, japo wasijue siku wala saa. Kama vile ambavyo tuonavyo tai wengi twajua kuna mzoga, vile vile tutajua kwamba Yesu yu mlangoni.

Yesu aliendelea kuwaambia yatakayotokea mamia ya miaka ya mbele. Ujio Wake utakuwa wa ghafla na usiotegemewa kwa wasiojitayarisha. Jua litatiwa giza au kupatwa, na mwezi hautaoa mwanga, hili lilitokea Oktoba 27, 1780, nyota zitaanguka, hili lilitokea Novemba 12 na 13 ya mwaka 1833, na nguvu za

mbinguni zitasikika, matetemeko kama lile la Lisbon la mwaka 1755, yote haya yametokea na yanaendelea kutokea. Ndipo itakapoonekana ishara Yake Mwana wa Adamu mbinguni, ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza wale waovu wakimwona anakuja mawinguni na utukufu mwingi. Naye atawatuma Malaika Zake, pamoja na sauti na nguvu na utukufu mwingi. Malaika watatumia sauti ya tarumbeta kuwakusanya wateule Wake waliomtumaini kutoka pande nne za dunia. Dalili hizi zote za Mathayo 24 zimetimia isipokuwa moja tu, nayo ni habari njema kwenda duniani pote, na hiyo hufanyika kwa njia ya kumruhusu Mungu kuingia mioyoni mwetu. Kwa vile vita kuu kati ya wema na ubaya haimruhusu Mungu kuchukua mioyo na nia zetu kufanikiwa kwa jambo hilo zima kunategemea ukubali wetu.

Akasema "kwa mtini jifunzeni mfano, majani yake yakiisha chipuza na kuchanua, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno u karibu, basi mkiona haya mjue Yesu, Yu karibu mlangoni. Mbingu na dunia zitapita ila Maneno ya Mungu hayatapita kamwe. Yesu Anakuja, tufarijiane kwa habari hii njema! Maranatha! Hakuna aijuaye siku wala saa ila Baba aliye mbinguni. Watu wangejua siku au saa, wangeliogopa adhabu na kujitayarisha ila mioyo na nia zao zisingekuwa tayari kuwa raia wa mbinguni. Wangefika mbinguni na kuanza kuiba lami kwenye barabara, na kupigana na watu, na kwao mbingu ingekuwa jambo lisilofurahisha.

Kama ilivyokuwa siku ya Nuhu watu walijisahau na kuendelea na mahangaiko ya maisha kama kawaida, hata leo ni yale yale; watu wanakula, wanacheza dansi, wanachota maji, wanakunywa uji, wanasengenya, wanaangalia runinga, wanafua nguo, wanaosha vyombo, wanapiga deki, na kufagia, wanaenda shule, wanaenda vibaruani, wanaoa na kuolewa hata bila wao kutambua. Ndivyo itakavyokuwa siku ya mwisho kwa wale ambao wanajishugulisha mno na mambo ya dunia ya leo, bila kutafuta mambo ya kiroho, ya kujitayarisha kwa ufalme wa Mungu. Watu hawa waweza wasiue watu na kufanya mambo ambayo tungeita 'dhambi kubwa' ila mawazo yao, yatakuwa kwenye watu, vitu au mambo ambayo hayaokoi.

Watu wawili watakuwa shambani wakilima au katika shughuli zao, mmoja atakuwa tayari kutwaliwa, mwingine hatakuwa tayari na ataachwa. Wanawake wawili watakuwa wakifanya shughuli zao, na mmoja atakuwa mwumini na yuko tayari, bali mwingine atakuwa hayupo tayari. Itabidi kukesha siku hizo maana "hamjui siku ni ipi atakayokuja BWANA wenu." Endapo mtu angejua mwizi anakuja usiku, angekesha bila kulala, ili nyumba yake isivunjwe. Hata nasi leo tujiweke tayari, maana hatujui sasa ya Yesu kuja, maana katika saa tusiyodhani ndipo atakuja Mwana wa Adamu. Mtumwa mwaminifu aliyewekwa wakili na BWANA, ili awape watu chakula kwa wakati wake, itakuwa heri kwake BWANA Wake akija na kumkuta anafanya kazi aliyopewa.

Kazi tuliyopewa ni ya kuwaambia watu wengine, habari za hukumu kwamba, "watu wamche na kumtukuza maana saa ya hukumu" inaujia ulimwengu upesi. Mpendwa mtoto, Mungu anakuja kuhukumu dunia, twahitaji tuwe tayari sasa. Tusiwe watumwa ambao tunasema "BWANA wetu Yesu anachelewa kuja" tukaanza kuwa na roho mbaya tukiishi kwa anasa na kutofikiria wengine, hata kutesa watu

wanaompenda Mungu na "kuwapiga wajoli wetu, na kunywa pamoja na walevi." BWANA anakuja siku tusiyodhani, na saa tusiyojua, maana adhabu Yake ni ngumu, akasema ni "kukatwa vipande na kuwekwa kwenye fungu la wanafiki na ndiyo kutakapokuwa kilio na kusaga meno." Ila twaamini wale waliojikabidhi kwa Mungu, wakijitoa kihali na mali watajua mwisho u karibu, japo hawatajua siku wala saa.

Mitume walijua kwamba imani yao, lazima iwe imara, nasi pia, imani yetu lazima iwe imara. Je waweza kuwaambia wengine kuhusu ufalme Wake. Kama tunampenda Yesu, itakuwa jambo la kawaida tu kuitika wito Wake na kumpenda Yeye kwa kushika Maagizo Yake, kuwapenda wenzetu na kuwaambia habari njema za Ufalme. Tungependa arudi mapema. Tukio la kurudi kwa Yesu kutuchukua kwenda mbinguni, ndilo la muhimu kupita yote katika maisha yako na yangu, ambalo ungependa litendeke hata leo ikiwezekana. Hatuwezi kuogopa tukisema pia ndilo tukio kubwa na la kupendeza linalongojwa na sayari zote kila mahali kwenye milki ya Mungu! Hebu kuja kwa Yesu kusiwe kitu cha ghafla kwetu. Wengine wamefikiria wangemaliza shule ya msingi, au sekondari au chuo ndiyo twende mbinguni. Wengine wamefikiri wangeoa au kuolewa kwanza, au kununua nyumba au gari, au kufanya mambo fulani wanayoyapenda kwanza. Napenda kusema mbinguni kuna mazuri zaidi ya hayo tunayoyafikiria. Na hata kuwepo pale tu kutaburudisha mioyo katika namna ya ajabu kabisa. Tutasikia taabu zetu zote zimetoweka papo hapo. Huzuni, vilio, maumivu, kifo, chuki, na uovu wa aina zote havitakuwepo. Hakuna kupungukiwa kule, au majuto, yaani hutajisikia ukilaumu eti 'ningekuwa duniani kule ningefanya hivi au ningekuwa na vile kutatua tatizo langu'.

Mama mmoja rafiki yangu, aliyekuwa anategemea kupata mtoto nilipomwambia, "Yesu angekuja leo, ingekuwa furaha iliyoje kuachana na shida zetu." Alinijibu "wacha Yesu asije kwanza, nina miezi miwili tangu nijifungue, maana sikupata mtoto miaka mingi, basi nikishajifungua hapo ndiyo Yesu aje." Nilimwuliza, hivi Yesu akija leo, atamwua mtoto? akasema La! Nikamwuliza tena, kule mbinguni mtoto atakosa chakula, nguo au malazi? Akasema La! Nikamwuliza kule mbinguni kama utakosa pesa ya kumsomesha mtoto, au atakosa kwenda chuo kikuu? Akasema La!

Kweli mtoto asingekosa chochote, iwe ni mwanasesere, magari ya kuchezea, miti ya kupanda au watoto wa kucheza nao, watakuwa wengi kule. Nikamwambia, sasa mbona yote kule ni mazuri kwa mtoto kuliko hapa! Akastaajabu akasema "sikufikiria jamani, kumbe yote ni mazuri! Wacha aje hata leo." Mama huyu alijifungua mtoto aliyemngojea kwa miaka mingi, maana alikuwa na tatizo la kutopata mtoto, kwani watoto wengine mimba zilitoka, na wengine walikufa. Akafurahi alipopata mtoto. Ila mtoto alipozaliwa alikuwa na shida ya mizio ya mambo mengi, kama vile moshi, nyama, maziwa, ngano mahindi, mayai, karanga na jamii zake, na orodha iliendelea kuwa ndefu. Walikuwa hospitalini mara nyingi kwa maradhi haya, ila sasa hali inaendelea kuwa nzuri. Ilibidi akinunua kitu akisome, na amwonjeshe mwanae kipande kidogo cha chakula kama majaribio, ndipo ampe ili isilete shida kubwa. Mtoto alipoenda shule ikawa ni shida akipewa chakula na watoto wenzake, mara mwili unavimba na anashindwa kupumua vizuri, kisha wanamkimbiza hospitali na kumpa sindano na dawa analazwa. Je haya yangetokea tungekuwa mbinguni? La! yasingetokea. Dalili za kuja kwa Kristo, Biblia imezieleza kwa undani, ni nyingi

nazo ni kuongezeka kwa maarifa na watu kwenda huko na kule, Yakiwemo maarifa ya Neno la Mungu.

Ile safari ya kwenda mbinguni itakuwa ya ajabu sana, kwani tutasafiri na kuona nyota, mwezi na vingine vingi tukiwa njiani. Tunavyoona wanaanga wa roketi za kwenda mwezini wakisafiri, sisi tutasafiri wenyewe kwa miili yetu tutainuliwa na kutembea sehemu mbali mbali. Hatutalipa dola milioni tatu kama wengine wanavyolipa siku hizi wanavyofanya kwenye kampuni ya Elon Musk. Yawezekana uone kama ni ndoto au sinema, la hasha, mwanzilishi wa sayansi ni Muumbaji Mwenyewe Ndiye amesema, na hivyo tunaamini, kwa vile hakuna alilosema lisitimie. Yote asemayo ni ya Kweli kabisa. ila ni lazima tuwe wavumilivu mpaka mwisho wa safari.

Matetemeko kama lile la Lisboni Ureno la mwaka 1755 likasikika mpaka Greenland, Morocco na nchi zingine, kuanguka kwa nyota mwaka wa 1833, jua kutiwa giza mwaka 1780 hata mifugo ikarudi nyumbani asubuhi za saa nne, ni mifano michache ya yale yaliyotimia, na yanaendelea kutimia leo kama vile Tsunami ya Indonesia. Matetemeko yanatokea zaidi hata kwa maelfu kwa mwaka mmoja siku hizi. Matukio haya yametoa shauku ya watu kujisomea zaidi kuhusu unabii. Wengine wamejikita kwamba vitabu vya unabii kama Daniel na Ufunuo, au unabii karibu wote ulishatokea zamani, kuanzia wakati wa kuharibiwa kwa Yerusalemu 70 na wakati wa kuanguka kwa himaya ya Rumi. Na wengine wamejikita kusema kwamba matukio yote ya unabii isipokuwa machache yatakuwa siku za mwisho.

Yote mawili si kweli, hivyo Chukua muda ujisomee na utaelewa vizuri kwani mtoto wangu wa miaka 10 tuliposoma naye Biblia na miongozo kama Amazingfactsprophecy, AmazingdiscoveryTv na MyBiblefirst/MyBibleguides tulielewa vizuri kuhusu tarehe za matukio ya unabii katika sura hizi. Neno la Mungu linahitaji Roho Mtakatifu na kiu/shauku tu na hata mtoto atalielewa vizuri. Tunajaribiwa kufungua maombi ya wale wanaohitaji Biblia ili kuwawezesha watoto kuwa na Neno la Mungu mikononi mwao. Unabii wa Danieli 2 na 7 uko wazi, ukienda kuusoma kwa kumwomba Roho Mtakatifu na kusoma historia ya dunia, kamwe hautapotea. Kitabu cha Ufunuo kimefungua kitabu cha Danieli, ukienda kusoma zaidi Ufunuo 13 na 14 kuhusu imani za Kweli na za uongo (Mwanamke mkamilifu na Kahaba) utaweza kuona zaidi kwa kina. Ni ombi letu kwamba kila nyumba itakuwa na Biblia angalau moja! Na walio na zaidi wanaweza kugawia wengine. Nchi nyingi vijijini hakuna Maandiko, ila mtandao umesaidia kwa kiasi fulani tuwe na Maandiko, japo Biblia ya karatasi itafanya ujifunze kwa kina zaidi! Ndivyo tunavyodhani, hata hivyo hatujui kama umeme na teknolojia itasuasua siku zijazo!

Teknolojia ina mengi maovu ila ina mengi mazuri pia, ni jinsi unavyoitumia, ukijihadhari kutopoteza muda. Adui anapoitumia teknolojia, Mungu Naye anaitumia hadi mwisho wa wakati. Unabii huu upo kwenye historia ya dunia na pia upo kwenye Biblia, na leo upo kwenye kompyuta na simu zetu. Siku hizi waweza kutengeneza gari, kupika vitumbua, kutibu maradhi fulani kwa msaada kutoka mitandaoni (kugoogle tu!) tunaishi katika ulimwengu wa dotcom. Hata google imekuwa tendo (verb). Ila Mwombe Mungu utumie teknolojia kwa utukufu Wake kuelewa kwamba siku tulizo nazo ni chache kujiandaa na kuandaa wengine.

Daima kumekuwa na vita dhidhi ya Neno la Mungu. Shetani anajua binadamu akilipata atajua Mungu ni mwema naye ni mwovu asiyefaa, hivyo Neno la Mungu limefichwa kwa vipindi vingine na kuwa nadra sana. Ila Mungu ashukuriwe kwamba Biblia ndiyo bado kitabu kinachouzwa kuliko vingine vyote (bestseller). Ndicho kilikuwa kitabu cha kwanza kuchapishwa pia. Habari njema kuhubiriwa inatimia kila kukicha kwani toka John Wycliffe aliyeitwa nyota ya matengenezo (Morning star of Reformation miaka ya 1300) aliponuia kwamba Neno la Mungu Biblia lazima iwe mikononi mwa watu, hata wale wasiosoma sana mashambani, Mungu amelitimiza Neno Lake. Wycliffe alitafsiri Biblia toka kilatini, lugha isiyozungumzwa leo hii, au kama wengine wapendavyo kuiita lugha iliyokufa kwenda kingereza.

Siku hizo nchi hizi zilitawala dunia kama vile unabii wa Danieli 2 na 7 unavyosema kwamba nchi 10 za ulaya zitatawala dunia. Huyu alipokewa na wengine kama William Tyndale aliendelea kuandika na kuchapa, Martin Luther naye akatafsiri Biblia kwenda katika Kijerumani na kuwawezesha watu wa kawaida wasome Neno la Mungu. J. Guternberg naye akawa ameshatengeneza mtambo wa kuchapa, habari njema ikazidi kusonga mbele.  Soma zaidi historia ya kupata Biblia yetu ya Kiswahili iliyotoka Ujerumani na Uingereza. Rudia tena unabii wa Daniel 8:14 na Daniel 9. Uone jinsi ambavyo mambo mengi yametimia.

*Omba kwa Imani Isiyotetereka — Omba, ndio, omba ukiwa na imani isiyoyumbayumba na  amini. Malaika wa agano, yaani Bwana wetu Yesu Kristo, Ndiye Mpatanishi na Mwombezi anayesimamia kukubaliwa kwa maombi ya waamini Wake.
-------------------------

Maswali: Kwa nini Yesu hakutuambia siku au saa anayokuja? Tufanyeje ili siku ile ya kuja kwa Yesu isitukute kama mwivi? Tutajuaje kuwa huyu si Kristo? Siku zetu zimekuwaje kama za Nuhu? Tutatofautishaje miujiza ya uongo na ya Kweli ya Mungu?

**SIKU YA 266.**
**(Septemba 22)**

# Wanawali watano wajinga, na watano werevu.

**Mathayo 25**



Wakati huu wa mwisho unafananishwa na wanawali kumi waliochukua taa zao kwa furaha, wamngoje bwana arusi aliyekuwa anakuja kwa bibi arusi usiku, kabla ya sherehe kuanza. Wanawali watano walikuwa wana busara na watano walikuwa wapumbavu. Wanawali hawa wanasimama badala ya washiriki wote au waumini wa wakati huu wa mwisho kwani wote walikuwa mabikira yaani makanisani. Siku zile ni bwana arusi alikuwa anangojewa kwa siku kadhaa, huyo ndiye alikuwa kiini cha arusi. Siku hizi huwa tunamngojea bibi arusi kuja mwishoni na kunyanyuka akiingia. Wanawali hawa wote walipiga usingizi, ila wale watano walijirudi, japo walirudi nyuma, walishtuka na kuanza njia bora tena.

Hawa walikuwa na mafuta ya kutosha kwenye taa zao, ila watano walikuwa wapumbavu, walikuwa na taa bali walisahau kuchukua mafuta ya kutosha. Usiku wa manane kukawa na kelele za shamra shamra, kwamba bwana arusi ameingia waende kumlaki. Wanawali wote walitengeneza utambi wa taa zao, na wale wapumbavu wakawaomba wale wenye busara mafuta kidogo, maana taa zao zilikuwa zinazimika. Wale wenye busara, walisema hawawezi kwani "hayatatutosha sisi na ninyi" bora mwende dukani, mkajinunulie. Sidhani kama maduka yalifunguliwa usiku wa manane kama siku hizi, ambapo maduka mengine yanafunguliwa kwa masaa 24. Wakienda kununua mafuta usiku huo, kwa hofu na haraka pengine kwa marafiki wenye maduka yao binafsi, mara Bwana arusi akatokea nao waliokuwa tayari, wakaingia pamoja Naye arusini.

Wakaja wanawawali wale wapumbavu na kuomba wafunguliwe mlango, ila walikuwa wamechelewa na bwana arusi alisema "siwajui ninyi." Basi ni muhimu kwa kila binadamu kukesha, maana hatujui saa na wakati wa Yesu kuja, lazima tuwe makini kujitayarisha kwa kuja kwa Mwana wa Adamu. Tukijishughulisha na masumbuko na mambo mengi ya dunia katika maisha yetu, hatutakuwa tayari wakati Yesu atakapotokezea mawinguni. Mitume walifikiria mfano huu una maana

gani, nao wakaelezwa, mafuta ni Roho Mtakatifu, na Yesu ndiyo Nuru ya dunia. Roho Mtakatifu Ndiyo mafuta yale ya ziada, yanayowasaidia watu kumngoja Yesu arudi tena, kama vile BWANA arusi alivyongojewa. Yesu kwenye Maandiko ni Mfano wa BWANA arusi na kanisa au waumini ndiyo bibi arusi.

Wale wanawali 10 wanawakilisha wale wanaongojea kuja kwa Yesu mara ya pili duniani. Kwa vile umepita muda mrefu bila Yesu kurudi watu wanarudi nyuma na kuanza kulala usinginzi kwa mambo ya muhimu ya imani. Wamesahau kwamba inawabidi kukesha kama BWANA wao alivyowatuma na kuwaambia wengine upendo wa Yesu. Wanapaswa kuwaambia majirani zao, na wao wenyewe kujitayarisha. Watumishi wanaongoja BWANA arusi wanakuwa tayari, kufungua mlango akija, kisha watafurahi kwa ile karamu aliyowaandalia, yaani tuliyoandaliwa binadamu wote. Lazima tuwe tayari maana hatujui saa wala siku, Yesu angetuambia saa au siku ajayo, huenda wengi wangefanya mambo yasiyofaa, wengine wangefanya mambo kwa woga, kwa vile wanataka kwenda mbinguni, ila mioyo yao isingekuwa na upendo wa Kweli.

Wametokea watu mbali mbali, waliosema Yesu alisema hakuna ajuaye siku wala saa ila mwaka tunajua. Hawa watu wameacha kusoma shule, wameacha kazi, wakauza vitu vyao wakimngojea Yesu. Hili ni kosa, Yesu alisema tuendelee kufanya shughuli zetu na kupanga mipango yetu awe anakuja leo au kesho. Hakusema tuache kufanya shughuli zetu za kila siku au tuache kuwaambia watu juu ya kuja Kwake. Kama shuguli zetu si dhambi, kwanini tuziache, nasi ni binadamu, yabidi tulime, tuvune, tule n.k Wale wenye mafuta ni wale wenye imani, mafuta ni Roho Mtakatifu anayetusaidia uzoefu wa tabia ya mbinguni, uzoefu ambao hakuna mtu aweza kumwomba mwingine. Roho Mtakatifu Ndiye anatusaidia binadamu kuwa na imani ya kutosha kumsubiri Yesu wakiwashuhudia wengine. Yesu atakapokuja waaminifu wataingia katika ufalme wa Mungu.

Somo kubwa hapa ni kwamba tuwe daima tayari kwa kuja kwa Yesu mara ya pili, tukeshe na kuomba, kwa vile hatujui Yesu anakuja lini. Tuangalie dalili alizosema, na ishara za nyakati, ili tusiwe kama wale wanawali wajinga. Hakuna anayeweza kuingia mbinguni kwa matayarisho ya mwingine. Wanawawali werevu wasingeweza kuwagawia wajinga Roho Mtakatifu anayefanya kazi katika maisha yao, au uzoefu wao wa imani na tabia. Kujitoa kikamilifu yaani kujisalimisha kwa Yesu, ndiyo ufunguo wa kuingia mbinguni.

*Umealikwa kuja, kuomba, kutafuta, kubisha; na umehakikishiwa kuwa hautatoka mtupu/bure. Yesu anasema, “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye hupata; na yeye abishaye atafunguliwa.”

---------------------------

Maswali: Wanawali watano wajinga wote ni washiriki na waumini leo, tofauti yao ni nini? Wanawali watano werevu ni sawasawa na watu gani leo? Je, mafuta yanawakilisha nani leo? BWANA arusi aliyeandaa karamu ni nani? Mtu afanyeje ili aingie karamuni?

**SIKU YA 267.**
**(Septemba 23)**

# Kutumia talanta zetu ili ziwe na faida.

**Mathayo 25.**



Yesu akijua ataondoka, aliendelea kuwapa mitume Wake wosia, ili wajue cha kufanya watakapokuwa wenyewe. Akatoa mfano wa hali ya siku za mwisho itafanana pia na mfanyabiashara aliyetaka kusafiri na aliwaita watumwa wake, akawekeza mali zake kwao kama mawakili. Wa kwanza alipewa talanta za fedha tano, wa pili mbili na wa tatu moja, kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake, akasafiri. Ndipo yule wa kwanza alienda kufanya biashara na zile talanta tano bila kukawia, nazo zikazaa kumi. Na yule mwenye talanta mbili alichuma faida ya talanta mbili na zikawa nne. Yule wa talanta moja alienda akaifukia chini, ili kuificha ile fedha ya bwana wake. Baada ya siku nyingi, huyu bwana alirudi na akwauliza watumwa hawa, na kufanya hesabu nao. Yule wa tano akahesabu na kueleza faida aliyoleta ya talanta tano "Tazama uliweka kwangu talanta tano; tazama, talanta nyingine tano nilizopata faida." Yule bwana akasema "vyema mtumwa mwema, na mwaminifu, ulikuwa mwaminifu kwa machache, nami nitakuweka juu ya mengi, ingia katika furaha ya bwana wako. Yule wa mbili akatoa hesabu kwamba amezalisha talanta mbili tena, basi naye akaambiwa vyema pia, ila yule aliyefukia talanta yake moja, alirudi nayo ile ile akisema "bwana nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya, basi nikaogopa, nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi, tazama ndiyo hii iliyo yako."

Bwana wake akamwambia "wewe mtumwa mbaya na mvivu, ulijua kwamba navuna nisichopanda, nakusanya nisipotawanya, si ungeiweka hiyo fedha yangu kwa watu

ambao wanatoa riba, ili nikija ningalipata iliyo yangu na faida pia." Basi yule bwana alitoa amri, yule mtumwa wa talanta moja ya fedha anyang'anywe ile talanta na apewe yule mwenye kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele, lakini asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa. Na yule mtumwa asiyefaa atatupwa katika giza nje ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno. Mfanyabiashara kwenye mfano huu ni Yesu, alipokwenda aliacha mitume, na sisi sote binadamu alitupa talanta kutokana na uwezo wetu wa kuzizalisha. Wengine wana talanta tano, wengine mbili na wengine moja. Hakuna binadamu asiye na talanta, waulize wazazi wako na marafiki, watakuambia talanta yako ili uikuze. Kuna utafiti wa kujua talanta zako kwa kujibu maswali fulani. Pengine unaweza kuimba, au unapenda hesabu, pengine unashika mambo kichwani haraka na kukariri mafungu, pengine unacheza chombo cha muziki na kuelewa noti inayochezwa. Kaa mahali kidogo na anza kufikiria, talanta zako, usiseme huna.

Mara nyingi wengi hawajui talanta zao, ila unaoishi nao wanaziona. Zitumie hizo vizuri, kama ni tabasamu, kwa wale wenye huzuni, usizike talanta hiyo, hata kama ni moja itumie nayo itazaa. Ukifanya hivyo unaweza kukuta siku moja unazo kumi, kwa vile ile moja ilizaa. Ubaya ni kuizika, kuwa mvivu, au kukata tamaa. Kwa talanta hiyo moja uliyonayo kinachojalisha ni uaminifu wa kuitumia. Kuwa tayari BWANA ajapo ni kuchukua majukumu ya kufanya vitu vitakavyompendeza ajapo. Mungu hatazamii wewe kuwa na matunda mengi kama Sadiki au Neema, bali itategemea na talanta zako alizokupa.

Mtu asiye na kisomo bali anataka kujifunza kumtii na kumfanyia kazi BWANA atashangaa atakavyotumika na kubariki wengine kuliko hata wale wenye visomo na mali. Mtu mmoja ambaye namkumbuka ni Thomas Jefferson, aliyekuwa na miaka 32 alisomea sheria kwa wiki sita, naye akashiriki katika kutunga katiba ya Bunge la Marekani. Siku hizi kuna wanasheria wengi ambao wamesomea udaktari wa sheria ila hawajahusika kwenye miradi mikubwa kama hii. Uwezo wa kuzungumza pia ni talanta, twapaswa tuzungumze maneno vizuri, ili yaeleweke. Na kuvuta pumzi inavyotakikana. Sauti zetu zina mvuto kwa watu, tunapowaambia habari njema za ufalme wa mbinguni. Tusizungumze mambo yasiyo na maana, au kusengenya watu, huku ni kutumia talanta zetu vibaya. Kuanza kuwatesa watu wa Mungu makanisani, nyumbani au kwenye shule zetu na kusema kwa nini BWANA wangu anachelewa ni dhambi. Jinsi tunavyoishi na kufanya mambo, inaleta mvuto wa aina fulani kwa wale wanaotungalia. Kuwahi shuleni, kupanga vitu vyako vizuri na kuondoka mahali saa zinazotakiwa haya yote ni muhimu katika talanta ya muda ambayo kila mtu amepewa. Na ndiyo maana Martin Luther mwanamatengenezo wa Ujerumani alisema, twahitaji kuisikia injili kila siku, kwa vile tunasahau injili ni nini kila siku, na tunapaswa kujifunza jinsi ya kuihubiria mioyo yetu kila wakati.

Hakuna dhambi kubwa kama watoto wasio na kitu cha kufanya, maana kukaa bure bila kufanya kitu, kunafanya watoto wasiwe na manufaa (useless) wakiwa watu wazima na kualika. Watakaa kivivu, wakitengemea kulipwa hili litawakosesha ajira maana wengi wanatupima kwanza. Wengi katika maisha wangekuwa mbaraka mkubwa ila wameharibiwa na kukaa bila kazi ya kufanya. Hii imewafanya waingie katika mitego ya Shetani, kwa vile mawazo yao yalikuwa hayana chochote bora.

Biblia yasema mkono wako ukikuwezesha kufanya lolote, fanya kwa nguvu au uwezo wako wote.

Afya zetu pia ni talanta kubwa, maana tukiwa na afya na nguvu, bongo zetu zaweza kutofautisha mabaya na mema kirahisi. Tukiharibu afya zetu kwa vyakula vibovu kama vile vilivyokobolewa, vyenye sukari nyingi, chumvi au mafuta mengi na vileo hapo tutakuwa hatutumii talanta zetu vizuri. Tutaulizwa kwenye hukumu jinsi tulivyotumia talanta zetu. Mivuto tuliyonayo ni talanta. Pengine waweza kupendwa na watu, kuheshimika au watu wakikutazama wanatoa huduma kwa haraka, au kukusadia jambo. Hebu mvuto huo utumie kwa utukufu wa Mungu.

Pesa tunazopata ni talanta. Ni muhimu kuelewa Mungu Ndiye mpaji wa mali zote. Ubunifu wote na mambo yote tunayoweza kuyafanya ni Yeye anayetupa uwezo, iwe ni stadi ya kutengeneza kigari cha watoto au tabibu anayeweza kupasua mwili wa mtu na kusaidia kuondoa hitilafu ya moyo. Fedha ni kwa ajili ya mambo matatu tu, mahitaji yetu, mahitaji ya wenye shida na mahitaji ya kazi ya Mungu. Pesa haina thamani yoyote endapo haiwezi kusaidia mahitaji ya wenye shida na kuwa mbaraka kwenye kufanya kazi ya Mungu ili wengi waingie ufalme wa mbinguni. Je, kwa kidogo unachopata unarudisha zaka na kutoa sadaka?

Usingoje kufanya jambo moja kubwa kwa Yesu siku moja, matendo madogo madogo ya kila siku ndiyo yanajenga tabia. Yule mwenye talanta moja angeitumia vizuri, ingezaa na siku moja angekuwa na talanta zaidi ya moja. Kamwe tusifikiri kwamba tutashindwa. Tukishirikiana na Mungu Yeye hajawahi kushindwa. Mungu anaburudishwa endapo mioyo yetu ina ucheshi na upendo tukifanya vitu kwa shukurani kwamba ametuweka shambani Mwake, na siyo kwamba tutapata umashuhuri au mazao makubwa ya aina fulani.

Na siku moja Yesu atakapokuja atasema Maneno matamu kupita yote kwetu. Upole, ukarimu, utu wema, na kuhudumia watu ni talanta nzuri toka kwa Mungu. Kuwapenda watu fulani na kuwachukia wengine, si upendo wa kweli bali ubinafsi na ubaguzi. Tunangoja Yesu akija, atushike mikono na kusema "vyema mtumishi mwema ulikuwa mwaminifu kwa madogo, ingia katika raha ya milele." Hii itakuwa zawadi kubwa kupita zote duniani, ulizosikia, au kuzifikiri au kuzipata. Basi weka tahadhari talanta zako zizae.

*Kwa kuwa Kristo ni mfano wetu katika mambo yote, nasi ikiwa tutaiga mfano Wake kwa bidii, wa kuwasilisha maombi yasiyo choka na yenye bidii kwa Mungu ili tuweze kuwa na nguvu katika Jina Lake, Yeye Ambaye hakujisalimisha kwa majaribu ya Shetani, na akazipinga hila za adui mjanja, vivyo hivyo nasi hatutatekewa naye adui huyu (sisi nasi hatutashindwa na Shetani).


-----------------------------

Maswali: Kwa nini yule mwenye talanta tano na mbili walipongezwa? Orodhesha talanta unazoweka kuzitumia au kuzificha? Mfanyabiashara anafananishwa na nani? Kwa nini hata tukifikiri kuwa Yesu amechelewa ni vyema tuendelee kujitayarisha? Wewe leo unaficha talanta gani na kutumia zipi?

**SIKU YA 268.**
**(Septemba 24)**

# Pasipoti ya kusafiria Mbinguni.

**Mathayo 25**




Yesu akaendelea kuzungumza kwa mifano, akielezea visa au mambo ya kawaida, kuelezea mambo ya kiroho au ya ufalme wa mbinguni. Mifano au visa vilivuta usikivu maana vilikuwa vinafanya mawazo yao yawe na picha ya yale masimulizi. Mifano ilihusu maisha ya watu ya kila siku. Ilikuwa na mafundisho kwa kila mtu, pia ilikuwa ya kusisimua na iliyo rahisi kueleweka kwa watoto na hata wazee. Mwana wa Adamu atakapokuja, katika utukufu Wake, na Malaika watakatifu pamoja Naye, atakapoketi katika kiti cha utufuku Wake, atakusanya mataifa yote mbele Zake; Naye atatenga wale watu ambao ni Wake kweli, na wanamtii na kumtegemea Yeye, kama vile mchungaji atengavyo kondoo na mbuzi.

Atawaambia wale wa mkono Wake wa kuume "njoni nyinyi mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme, zawadi mliowekewa tayari tokea kuumbwa misingi ya ulimwengu. Kwa maana Nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; Nalikuwa na kiu, mkaninywesha, Nalikuwa mgeni, mkanikaribisha, Nalikuwa uchi, mkanivika, Nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama, Nalikuwa kifungoni mkanitembelea."

Wenye haki watashangaa kwamba walifanya haya lini, Naye atawajibu "amini Nawaambia, mlipowatendea mmoja wapo wa ndugu Zangu hawa wadogo wenye kuhitaji fadhili mlinitendea Mimi. Watu ambao walihitaji chakula mliwapa, na wale wasio na pa kuishi, mliwachukua kwenu na kuwafadhili, wale wasiokuwa na nguo mliwavika, wagonjwa mliwatembelea na kuwafariji, na wale waliokuwa jela hata magerezani hamkuwasahau. Yote mliyowafanyia wahitaji mlikuwa mnanifanyia Mimi."

Kisha akawambia wale walioko mkono wa kushoto, "ondokeni Kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake"; kwa maana Nilikuwa na njaa, msinipe chakula, Nalikuwa na kiu, msinipe maji ya kunywa, Nalikuwa mgeni msinikaribishe, Nalikuwa uchi, msinivike, Nalikuwa mgonjwa na kifungoni wala msije kunitazama. Wale waovu wakajibu "BWANA ni lini au wapi tulipokuona Wewe una njaa au una kiu, au u mgeni au uchi, au u mgonjwa au u kifungoni, tusikuhudumie?"

Naye atawajibu akisema kadiri msivyowatendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea Mimi. Hakumjali wengine hata Mimi najua hamwezi kunijali kwani ufalme Wangu ni wa kujaliana na kusaidiana. Sina uchaguzi bali kuwapa adhabu ya kukosa uzima wa milele. Bali wenye haki wataenda kwenye ufalme ule wa milele ambapo kila mtu anajali mwingine, maana wote ninyi ni watoto wa BABA mmoja. Akimaliza kusema haya ilikuwa imebaki siku mbili tu kuwa pasaka ile ambayo alisalitiwa na kusulubishwa.

Sura ya Mathayo 24 na 25 inaelezea mahubiri ya mwisho ya Yesu. Cha kushangaza katika mafundisho hapa, ni kwamba Yesu hatagawa watu kutokana na wanachoamini, bali kwa matendo yao. Yesu Ndiye mwamuzi wa mwisho, mimi na wewe hatuna mbingu zetu za kupeleka watu. Yeye Ndiye BWANA wa upendo wote, na mamlaka yote. Anatuambia kwamba hukumu yetu itatokana na jinsi tunavyowatendea wale ambao ni dhaifu kwetu. Masikini, yatima, wahitaji, wajane, wageni, waliobaguliwa na wote wa namna hiyo. Anasema makundi ni mawili tu, la mkono wa kushoto au la mkono wa kulia. La mkono wa kulia litaokolewa kutokana na upendo wao unaoonekana kwa matendo yao. Mungu atusaidie, tuombeane!

Tukisema kwamba tunamwamini Yesu nasi tuna nguo saba, na mwingine hana hata moja na hatufanyi mpango wa kumwambia mama au baba tutawasaidiaje hawa, tutakuwa shidani. Ufalme wa Mungu si wa kujifikiria sisi, au ubinafsi, na kutumia muda wote kwa ajili yetu. Ufalme wa Mungu ni wa kufaana, kujaliana, na si kujilimbikizia vitu, kuleta vitu kwetu vijae makabatini, na visitoke nje kusaidia wengine. Kutokana na mfano huu tunavyowatendea wengine ndiyo kibali cha kwenda mbinguni. Wale Mungu aliowasifia, wenyewe hakuwajua kwamba walikuwa wanahudumia watu, wakauliza ni wapi tulikufanyia haya? Watu hawa Yesu aliowasifu hawakujua theolojia au Mafundisho Makuu ya Biblia, ila walielewa kanuni za Mungu za upendo.

Wapo wengi hata leo ambao hawakujua Biblia ni nini, au Kristo ni nani, bali wana roho za huruma upendo na upole. Wamekuwa wakimwabudu Mungu bila kujua, japo

hawakupata kuwatia machoni Wakristo wowote kwenye maisha yao, kama zile nchi za milima ya Nepali, Burma au Tibeti wanasema kwenye nchi hizo asilimia 90% ya wakazi wake, hawajawahi kukutana na mkristo (1040 window.org au JoshuaproJect.org au theforgottenchristmas.org).

Hawa japo hawajui Sheria za Mungu au Maandiko Matakatifu, wamekubali maisha yao yaguswe na Roho Mtakatifu, maana Roho Mtakatifu hugusa kila binadamu, na kumpa nafasi aokoke. Roho aliyegusa anaonekana katika matendo na tabia zao, hawa watashangaa watakaposikia, kwamba ni watoto wa Mungu pia. Malaika pia ni wahudumu kama binadamu, ili watu waokoke. Nasi binadamu tuwaigize na tusirudi nyuma katika kuonyesha matendo ya huruma, kwa kujitoa kusaidia maana ni kitu cha thamani sana kwenye moyo wa Yesu.

Mungu anapotupa nafasi, mali au talanta, ni kwa ajili ya kusaidia wenye mahitaji, si kufanyia anasa zetu, kujilimbikizia au kuwapa wale ambao wanavyo vingi tayari. Pale ambapo karamu inafanyika, meza zikichafuliwa, na chakula mbali mbali, hebu kipikwe chakula rahisi ili masikini wasaidiwe kujikwamua kiuchumi kwa ujasilimali, hata kama tuna ardhi ndogo na mbegu. Kutoa makombo ya chakula kisicho na ladha au tusivyovipenda, nguo zilizotuchosha au kuu kuu, au chenji chenji za pesa zinazotuzidi na kuwapa wenye njaa, ni kujiangusha maana vitu hivyo duni hatuwapi wale watu bali tunampa Mungu Mwenyewe.

Kwenye miji wanapoishi wasio na makazi, walio magerezani na wale walio mahospitalini, ni mahali ambapo panahitaji msaada na matumaini. Kujali watu ni muhimu sana, na Mungu amekuwa mwaminifu kwani watu wa takwimu wanasema asilimia 80% ya utajiri wote duniani umo mikononi mwa Wakristo (Rich Christians in the World of Hunger, na Ron Sead). Tuweke tahadhari, wakati tunatoa vitu, mahali pengine mtu anafuja kununua nguo, na hazivai hata mwaka unapita, ila hataki kuzitoa, na akitoa hutoa zile zimepitwa na wakati anazozichukia sana, ila kabati limejaa nguo nyingi. Hata mimi napoandika, najikumbushia mambo haya, kwani hakuna aliyewasili, wote tupo safarini.

Yesu atakavyotokea mawinguni, pesa na mali zote zitakuwa hazina thamani, na zitatupwa barabarani na mtu asiziokote, kwa vile mbinguni kuna vitu vya thamani zaidi. Hata lami ya barabara kule ndiyo dhahabu, acha mbali na vito vingine, pengine almasi ndiyo itakuwa soli ya kiatu. Kundi la kushoto, litakuwa lile ambalo limehukumiwa kwenda Jehanamu kwa vile wamekuwa si watoaji wa muda wao, vitu vyao au upendo wao. Pengine walisikia mtu yuko hospitali na angepaswa kupewa dawa fulani apone, ila hawakufanya vile, kwa vile si jamaa yao hawakuwa tayari kutoa walicho nacho, basi itakuwa ni shida kwao. Jirani, yetu ni yoyote yule anayehitaji msaada wetu, haijalishi kwamba ni jamaa au siyo!

Je, unatembelea wagonjwa? Je, kuna mtoto shuleni hana rafiki na anahitaji uzungumze naye ili asiwe mpweke? Je, kuna mtoto hana chakula, nawe waweza kumgawia chako? Je, familia yako yajua wafungwa na watu wenye maumivu au mahitaji na mna uwezo kuwapunguzia maumivu hayo? Je, una nguo ambazo waweza kumpa mwingine ambaye ana moja tu? Fanya vile, maana hayo yote ni muhimu sana,

maana tukifanya hivyo tunamfanyia Yesu Mwenyewe. Picha inayopatikana hapa ni kuwa "watu watahukumiwa kutokana na kile walichokifanya au walichopuuzia kukifanya kwa watu ambao ni wahitaji au wenye maumivu."
Nakumbuka mama yangu alipoanza kutuambia, tutoe nguo zetu kwa wenye mahitaji kijijini nikiwa na miaka 6, ilikuwa ngumu; maana zingine tulitaka ziwe za makumbusho japo zilitubana! Hii yaonyesha twapasa tuombe ili Mungu atupe Roho Yake ya upendo na kutoa.


*Hakuna cha Kutuchepusha sisi kutoka kwenye Mafunzo ya Biblia na Maombi ya bidii — Usiruhusu chochote, hata uwe unakipenda kwa jinsi gani, kunyonya akili yako na mapenzi yako, kukukengeusha ili usisome Neno la MUNGU au kuwa maombi ya dhati na bidii. Kesheni mkiomba. Ishi maombi yako mwenyewe.
---------------------------

Maswali: Elezea kundi la kushoto na la kulia ni lipi? Kwa nini watu hawakujua kwamba wanamfanyia Yesu mabaya au mazuri? Je kuna nini wiki hii unachoweza kufanya kusaidia wenye shida? Waweza kufikiri sababu zinazowafanya watu wasisaidie wenye mahitaji japo wana uwezo wa kufanya vile? Je, nani kati ya watu hawa walikuwa wa dini waendao kanisani au wale wenye matendo ya upendo? Je, kuna mtoto anayeonewa au anayechekwa darasani ambaye wewe unaweza kumsaidia kwa njia fulani?

**SIKU YA 269.**
**(Septemba 25)**

# Yesu anamfufua Lazaro.

**Yohana 10 na 11.**



Yesu aliendelea kuhubiri, hata wengi waliamini. Kule Bethania, maili kama mbili kutoka Yerusalemu mjini, palikuwa na ndugu watatu, nao ni Martha, Mariamu na Lazaro, hawa walimkaribisha Yesu na wanafunzi Wake wakae kwao. Mariamu ndiye yule aliyempaka mafuta Yesu miguuni kumtayarisha kwa maziko Yake wiki moja hivi kabla ya Yesu kuuawa, Naye akasema alifanya yote aliyoweza! Basi huyo kaka yao Lazaro aliugua mno, na dada zake wawili walituma ujumbe kwa Yesu alipokuwa anahubiri Pebirea wakisema "BWANA Yeye umpendaye hawezi anaugua mahututi" njoo haraka. Yesu aliposikia aliendelea na shughuli za kuhubiri na kuwaambia wanafunzi "ugonjwa huu si wa mauti bali ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu, ili Mwana wa Mungu atukuzwe kwa huo."

Naye Yesu aliwapenda Martha, Mariamu na Lazaro, alisikitika kusikia kwamba Lazaro anaumwa, ila alikaa siku mbili zaidi pale alipokuwapo. Kisha baada ya hapo aliwaambia wanafunzi warudi Uyahudi tena, na wanafunzi wakamwambia "Rabi ni juzi juzi tu wayahahudi walikuwa wakikutafuta kukupiga kwa mawe, nawe unakwenda huko tena." Yesu aliwajibu kuna saa 12 tu za mwanga wa mchana, mtu akienda mchana hajikwai kwa sababu aiona nuru ya ulimwengu, ila akienda usiku anajikwaa kwa sababu nuru haipo. Alisema hivi akimaanisha huduma Yake haikuwa na muda, usiku ulikuwa umekaribia, Naye ataondoka.

Kisha akawaambia "rafiki yetu Lazaro; amelala lakini ninakwenda Nipate kumwamsha." Alikuwa ana maana usingizi wa mauti, maana Biblia huita mauti usingizi, mpaka siku ya ufufuo. Wanafunzi wakifikiri ni usingizi wa kawaida walishangaa alipowaambia Lazaro amelala, kwani watu hulala kila siku; ndipo akawafafanulia wazi wazi "Lazaro amekufa, Nami nafurahi kwa ajili yenu kwamba sikuwako huko, ili mpate kuamini; lakini twendeni kwake." Tomaso aitwaye pacha akasema wacha twende na Yesu kama watu wanataka kumwua kule Uyahudi, tuko tayari kufa pamoja Naye. Yesu hakuonekana kuwa na haraka, Naye aliwasili baada ya siku nne.

Yesu alipofika alikuta Lazaro amezikwa na kukaa siku nne ndani ya kaburi, na watu wengi walikuwa wamehudhuria kwa maana Yerusalemu ni mwendo wa nusu saa hivi. Wayahudi hata wale viongozi, walikuja kuhani au kuwapa faraja Martha na Mariamu. Jamaa na marafiki pia walikuwa pale. Na kwa desturi ya pale walikuwa wamekodi watu wanaolipwa kulia, pengine kuonyesha jinsi jamaa yao anavyopendwa "aliliwa sana ndugu yetu alipokufa, alipendwa eti." Vurugu na kelele zilikuwapo kwa ajili ya hali ile na Martha aliposikia Yesu anakuja alienda kumlaki nje kidogo ya nyumba, na Mariamu alikuwa ndani ya nyumba.

Martha baada ya kusalimia, neno lake la kwanza lilikuwa "BWANA kama ungalikuwako hapa ndugu yangu hangalikufa." Japo Martha alipenda shughuli, alimpenda na kumtumaini Yesu. Akaendelea kusema "Lakini hata sasa najua ya kuwa yoyote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupa." Yesu akamwambia "ndugu yako atafufuka." Martha alijibu vile ambavyo tunaelewa hata leo kwenye Neno la Mungu "Najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho." Martha alijua ufufuo kwa wote ni siku ya mwisho, makaburi yatafunguka na wafu watatoka na kuwa na mwili kamili wa kutokufa na kumlaki BWANA mawinguni. Hakuna mtu anayekufa na kwenda mbinguni moja kwa moja, isipokuwa Musa, na Yesu tu ndiyo walipitia njia hiyo.

Ndipo Yesu akamwambia, maana wengi walisahau na kumwona Yesu ni nabii na rafiki tu, bali Yesu akamkumbusha Yeye ni nani akisema "Mimi Ndimi huo ufufuo na uzima, yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa atakuwa anaishi. Naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je unasadiki hayo?" akamwuliza Martha. Martha akajibu bila mashaka "BWANA nimesadiki ya kwamba Wewe Ndiwe Kristo Mwana wa Mungu, Yule ajaye ulimwenguni."

Hapa ndipo Masadukayo ambao hawakuamini ufufuo na malaika walikasirika. Wao japo walikuwa watu waungwana na wazuri waliojua kumvumilia Yesu kuliko Mafarisayo walioiamini Biblia yote japo waliweka sheria zao kuwa kongwa kwa watu, walianza kukasirika sana. Masadukayo walikuwa kama wachungaji, na hili ni jambo la kutisha kwani Mchungaji asiyeamini ufufuo, wala kuwepo kwa malaika imani ya Mungu kwake huyo ni kama imekwisha! Maana Mungu anaweza kufufua, nasi sote tunategemea ufufuo vinginevyo imani yetu ni bure. Paulo ameelezea hili vizuri kwenye 1 Wakorintho 15, kama hakuna ufufuo dini yetu haipo! Masadukayo ndiyo walikuwa viongozi wa dini, au kanisa. Mafarisayo wao walikuwa na sauti kwenye Baraza la Sanhedrin la Waisraeli. Warumi wao hawakuwa na chuki na Yesu. Watu wa Mungu Mafarisayo na Masadukayo ndiyo walikuwa sumu ya ufalme wa Mungu.

Martha alipomwambia Yesu anasadiki kwamba Yesu Ndiye Kristo na Mwana wa Mungu, alienda kumwita dada yake Mariamu faraghani kwa kunong'ona, kwamba "Mwalimu Yupo hapa anakuita." Naye aliposikia hivi aliondoka upesi amfuate Martha, na Wayahudi waliokuwa pamoja walifikiri wanaenda kaburini kuomboleza kaka yao tena, wakamfuata walie Naye kaburini na wamfariji. Mariamu alipofika Yesu alipo, alianguka miguuni Mwake na kumsujudu akisema tena "BWANA kama ungalikuwapo hapa ndugu yangu hangalikufa." Yesu alipomwona analia Naye

akaugua rohoni, akafadhaika mno, na kusema mmemweka wapi Lazaro? Naye akalia machozi.

Fungu hili ndilo fupi pekee katika Biblia yote linalosema Yesu alilia machozi . Mwana wa Mungu akalia machozi, kwa ajili ya huzuni za watu, japo alikuwa anaenda kumfufua mfu na Yeye Ndiye ufufuo na uzima, bali alilia machozi. Wengi wanasema wanaume hawalii, au ukiwa mwanaume usilie, ila kulia kwa matumaini na kiasi, ni vyema kutuliza huzuni mioyoni mwetu na kuonyesha upendo wetu kwa mtu yule, kwa kutuliza hisia za huzuni. Yesu ni Mwanamume, tena Mwenye nguvu kuliko sisis sote, Naye akalia, japo alikuwa na uwezo wa kufufua, yaonyesha alikuwa anatulilia sote vizazi hata vizazi tutakaokufa siku zinazofuata. Alikuwa analilia zaidi hasa wale ambao watakaokufa kifo cha milele kwa ajili ya dhambi, kwa vile hawajamkubali Mwenyezi Mungu. Wale watakaokufa kifo cha milele kwa vile hawajamwamini Mungu, kwani mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele.

Wayahudi wengine wakaanza kuuliza "Huyu aliyemfumbua macho yule aliyezaliwa kipofu hakuweza kumfanya huyu rafiki Yake Lazaro asife kama angaliamua?" Kutoamini kwao kulimwumiza Yesu na akilia kwa huzuni, alifika kwenye kaburi ambalo lilikuwa ni pango, na jiwe limewekwa juu yake. Yesu akasema liondoeni jiwe, japo mwili ulikuwa umeoza kwa joto lile la jangwani. Yesu angeweza kuondoa jiwe kwa kutumia Malaika, ila kile binadamu anachoweza kufanya hupewa afanye, maana Mungu hupenda kufanya kazi na watu Wake. Hata leo, Malaika wangehubiri, na watu wangeokoka, ila ametupa kazi hii, wewe na mimi tufanye. Basi Martha akasema "BWANA ananuka sasa harufu itaenda kwa wote; maana ana siku nne toka amekufa" kweli kifo ni kifo, hata mpendwa tunayempenda inafika wakati ananuka, tunamwepuka, na inabidi azikwe. Yesu akasema "hivi sikukwambia kwamba ukiamini utaona utukufu wa Mungu?"

Basi Martha akaacha kuchambua mambo kwa kutumia uzoefu wake, bali akamwachia BWANA awaongoze. Watu waliondoa lile jiwe na Yesu akainua macho Yake juu mbinguni na kuomba "Baba nakushukuru kuwa umenisikia. Nami nalijua ya kuwa Wewe wanisikia siku zote; lakini kwa ajili ya mkutano huu wanaohudhuria nalisema haya, ili wapate kusadiki kwamba Ndiwe uliyenituma." Akiisha kuzungumza na Baba Yake Ambaye ni Baba yetu pia wa mbinguni aliita kwa sauti kuu "Lazaro Njoo huku nje." Wakasikia sauti ndani ya kaburi kama kuna mtu, na Lazaro akatoka nje toka kaburini, yule aliyekufa, akiwa amefungwa sanda miguuni na mikononi, na uso wake umefungwa leso, na watu wakapata hofu, maana alitisha kwa zile sanda alizofungwa.

Naye Yesu akawaambia "mfungueni, mkamwache aende zake." Basi kukawa na machozi ya furaha, Lazaro akiwakumbatia dada zake, Yesu, marafiki, jamaa na majirani. Hawa hawakutegemea kumwona tena, pengine walimgusa na kumwuliza, mtu akifa inakuwaje naye akasema ni kama usingizi hakuelewa au kutambua yanayoendelea. Yesu alibadilisha huzuni yao kuwa furaha, Lazaro hakuwa ameenda mbinguni, bali alilala kaburini akingoja ufufuo. Angekuwa yupo mbinguni na akarudishwa duniani tena, angesikitika, kwani ni nani atakayetolewa mbinguni aje

duniani na kisha afurahie jambo hilo? Hata kama ana dada wenye upendo kama Martha na Mariamu asingependa kuja na kuona hila za Mafarisayo. Hata hivyo angependa sana, mwezi unaofuata, awe na rafikiye Yesu anapofufuka mbinguni milele zote!

Watu wengi katika nchi zingine wamesema walikufa wakarudi tena na wakasimulia jinsi walivyokuwa wanawaza walipokufa, na jambo hili limeitwa 'near death experience' NDE, jambo hili haliendani na mafundisho ya Biblia, kwani mtu akifa hawezi kuwa na fahamu tena, hata Lazaro na wengine waliofufuliwa katika Biblia hawakusimulia visa kama hivi, kwani kifo ni usingizi, na mtu anakuwa hana fahamu kabisa.

Muujiza huu ulifanya maadui wa Yesu wachukie, maana wengi walimwamini Yesu kupitia muujiza huu. Marafiki na ndugu wa viongozi wa Kiyahudi waliona kwa macho yao kufufuliwa kwa Lazaro, na habari zikaenea kama moto kwenye majani makavu. Masadukayo ambao walikuwa hawajaleta chuki ya kuonekana au ya kutisha kwa Yesu, walipoona haya, kwa kuwa hawakuamini ufufuo, walisema Yesu anapaswa kufa japo hakuna hata mmoja alishuhudia baya alilotenda katika maisha Yake yote. Waanzilishi wa dini zingine wanakiri, na hata wafuasi waliowaona wanasema kwamba walivunja Amri za Mungu. Hata hivyo, Yesu hakushuhudiwa katika maisha Yake akitenda dhambi.

Kuhani mkuu na wenzake ambao wengi wao walikuwa Masadukayo wakaita mkutano wa baraza lao, na kusema kwamba kutakuwa na uasi wasipomshugulikia Yesu kwa kumuua. Wakasema uasi huu utafanya Warumi kuwanyima uhuru waliopewa. Kayafa alitabiri kama mtu wa mataifa, kwamba imempasa mtu mmoja kufa ili taifa lote lisipotee. Katika Sheria ya Mungu mtu hakutolewa kafara ila Yesu tu, alitolewa. Hivyo Kayafa bila kujua alikuwa anatabiri jambo la Kweli, kwamba Yesu atakufa, ili watu waokolewe kutokana na kifo cha milele. Yesu aliposikia haya alienda milima ya Efraimu. Hili ni jambo la ajabu kwetu, jinsi walivyomchukia Yesu na hata kupanga kumwua. Mtu aliyewasaidia na kuja kufa kwa ajili yao.
Kweli moyo ni mdanganyifu, ni nani anayeweza kuujua? Basi tuombe maana hata sisi tunamsulubisha Yesu tunapotenda uovu, na kufanya yale tunayopenda ambayo si mema.

*MUNGU Anajibu Maombi ya Dhati — Ni pale tu tunapoomba kwa maombi ya dhati, ndipo MUNGU atatupatia haja za mioyo yetu.
--------------------------

Maswali: Dada wawili walituma ujumbe gani kwa Yesu? Tomaso alionyesha ujasiri gani? Je Yesu alikuwa na marafiki wengine wa karibu zaidi ya wengine? Kwa nini Yesu alilia alipofika kaburini, japo alikuwa anaenda kumfufua Lazaro? Kwa nini Lazaro hakutokea mbinguni alipofufuka bali kaburini? Unafikiri Lazaro alipotoka nje ya Kaburi alimwambia nini Yesu? Kayafa alitabiri nini?

**SIKU YA 270.**
**(Septemba 26)**

# Wanapanga kumwua Yesu

**Yohana 11 na 12**



Basi wengi katika uyahudi waliokuja kwenye mazishi na kuona yale yaliyofanyika, yaani Lazaro alifufuliwa, wakamwamini Yesu. Maana wale aliowafufua tu waliokuwa wamekufa, waliamini wamezimia tu na baada ya siku tatu ndiyo walisema 'roho ya mtu hutoka', ila huyu alikaa kaburini siku nne. Watu wengine wakaenda kwa mafarisayo kuwaambia, na kuwachochea chuki. Basi wakuu wa mafarisayo na makuhani walifanya mabaraza, wakisema "Tutafanya nini? Maana mtu huyu afanya ishara nyingi na miujiza ya Kweli kabisa, tukimwacha hivi, watu wote watamwamini na Warumi watakuja na watatuondolea mahali petu na taifa letu.

Kuhani Kayafa ambaye ndiye aliyekuwa kuhani mwaka ule, akichukua kiti toka kwa baba mkwe wake kuhani Anasi aliyestaafu, alitabiri bila kujua kwenye hiki kikao akisema "Je hamjui, kwamba mtu mmoja ni lazima afe kwa ajili ya watu wote ili taifa zima lisiangamie" alisema haya kwa vile alikuwa mwanasiasa wa kanisa. Na Neno hili yeye hakulisema kwa nafsi yake, bali kwa kuwa alikuwa kuhani mkuu

mwaka ule alitabiri yale yaliyoandikwa kwenye Maandiko kwamba Yesu atakufa, si kwa ajili ya taifa hilo la Israeli tu, au Wayahudi bali kwa kila mtu amwaminiye duniani ili awakusanye watoto wote wa Mungu waliotawanyika ili wawe wamoja. Twapasa kujua Kifo cha Yesu si mwisho wa maisha Yake. Yesu alikuja afe ili atoe maisha Yake kuwa kafara kwetu, ili tusamehewe dhambi. Ni kwa kufa Kwake na kufufuka ndiyo aliweza kuokoa watu. Kifo cha Yesu ndiyo kiini cha injili. Lakini Yesu kama angekufa na kukaa karibuni isingesaidia, Ashukuriwe Mungi kwani Yu hai leo, kwa maombezi na kutupatanisha na Baba Yake!

Basi toka siku ile walifanya shauri la kumwua, na kupanga njia za makini. Na hivyo Yesu hakutembea tena kwa wazi kati ya Wayahudi bali alitoka na kwenda mahali karibu na jangwa mji uitwao Efraimu akakaa kule. Ulikuwa umekaribia sana wakati wa pasaka ya Wayahudi, yaani sikukuu iliyoanza wakati wa kutoka Misri kwenye utumwa. Nafikiri haikuwa bahati nasibu kwamba Yesu alikufa wakati wa pasaka, bali mpango wa Mungu kuonyesha kwamba YeyeNndiye pasaka Wetu Mwana-Kondoo wa Mungu achukuaye dhambi zetu, ili tupone kifo.

Ni muhimu kujua waandishi, mafarisayo, wazee na makuhani walikuwa viongozi wa kiroho. Makuhani wanaitwa wachungaji na maaskofu leo kwenye makanisa, au nyumba zetu za ibada. Hawa ndiyo walikuwa mstari wa mbele kumwua Mwana wa Mungu. Cha kujifunza hapa ni kwamba kuwa mtu wa dini si kibali cha kwenda mbinguni au kuwa mtu wa Mungu. Kuna watu wengi wanajiita watu wa Mungu ila wako mbali sana na Mapenzi Yake. Je, Mapenzi Yake ni nini? Maana walielewa Neno la Mungu kuliko watu wa kawaida. Je walifanya lipi baya ambalo sisi twapasa tuliepuke? Nafikiri unafiki na kiburi ilikuwa ndiyo shida iliyofanya wasifikiwe na injili.
Leo sisi tuna bahati zaidi yao kwa vile tuna Maandiko Matakatifu. Siku zile watu wachache walikuwa nayo, na wachache walijua kusoma; leo kila mtoto apaswa kuwa na Biblia, kama huna mwombe Mungu akusaidie kupata. Ana uwezo wa kukupatia, mpe muda na kwa wakati Wake utapokea. Biblia ni kama dola 10 hivi kuna vingine ambavyo ni ghali zaidi ya hiyo. Mwombe Mungu, akupe Roho Wake Mtakatifu ili uelewe Mafundisho Yake, maana yana uzima wa milele. Yaani utamjuaje kama husomi Neno Lake? Neno la Mungu si kitabu cha kawaida cha habari, ila cha mabadiliko ya maisha. Amini yale yaliyoandikwa, yathamini, kisha yatende. Neno linajibu maswali yote makuu ya maisha. Mungu amejifunua kwenye Neno kwa watu, ni safari ya historia ya mahusiano ya Mungu na watu Wake. Mwombe Mungu upendo wa Kweli Kwake Yeye na kwa watu, maana moyo una ugonjwa wa kufisha na ni mdanganyifu kupita vyote, ni nani aujuaye Kweli, isipokuwa Mungu.

Kuna viongozi wa kiroho wengi wacha Mungu, na ni msaada mkubwa kwa mengi kama kufundisha watu Neno, mashauri, huduma na mengineyo. Usichanganye kati ya mahusiano yako na Mungu au maagizo ya Neno la Mungu na maneno ya viongozi wako wa kiroho. Mungu na Mafundisho Yake ndiyo nambari moja, kisha viongozi wa kiroho. Matendo 5:29 inasema "imetupasa kumtii Mungu kuliko mwanadamu." Soma Maneno ya Mungu na kama huelewi, omba uelewa na uyatii. Usichukue mapokeo ya watu fulani kwamba babu aliamini tambiko au bibi aliabudu chini ya mti huu. Jiulize Neno la Mungu linasemaje? Soma Mathayo 23 jinsi viongozi wa kiroho

walivyoishi, wakiwapoteza wengi. Kila mtu atauchukua mzigo wake mwenyewe siku ya hukumu. Usiseme kwamba hukujua, maana maisha ya Yesu yanatuonyesha kwamba kila mtu anapaswa kumsikiliza Yeye kwanza kisha viongozi wa kiroho kama wachungaji, walimu au manabii. Dhehebu lako siyo kipaumbele cha kwanza bali Mungu na Maandiko Yake. Haijalishi upo dhehebu gani au dini gani.

Wengi wakatoka mashambani waende Yerusalemu wajitakase kabla ya kuhudhuria sikukuu hiyo. Wakuu wale wakasemezana "mwaonaje haji kabisa siku kuu hii?" Wakuu wa makuhani walikuwa wametoa habari au notisi na kuwaambia watu "anatafutwa Yesu, mkijua alipo, mtuleteeni habari ili tupate kumkamata." Hata ndugu Zake walimsukuma aende akajionyeshe kwa watu, wakahoji kama anataka watu wamjue kama Masihi, mbona anajificha? Pengine walitaka ajitwalie ufalme, nao kama ndugu wangefurahi kwamba kaka yao ni mfalme. Watu wengi Wayahudi walivyopata kujua kwamba Yesu atakuwa kwa Simoni mkoma alipoalikwa, walijikaribisha pale. Hapa ndiyo Mariamu alimpaka Yesu marhamu ya thamani nyingi kwenye miguu Yake. Wale wakuu walipanga kuja na walifanya shauri ili wamwue Lazaro yule aliyefufuliwa katika wafu, ili kuondoa ushahidi wa ufufuo. Kwa ajili ya Lazaro Wayahudi wengi walianza kumwamini Yesu kwa wingi, na kujitenga na uovu wa viongozi wa dini. Ilikuwa imebaki pungufu ya wiki sasa Yesu afe kwa ajili ya dhambi zetu. Yohana 20 yasema Neno la Mungu limeandikwa ili tupate kumjua Mwana wa Mungu na kwa kumwamini tuwe na uzima wa milele kwa Jina Lake. Si kwa jina la ndugu, au viongozi, mpendwa litilie hili maanani na kulipigia mstari. Ni kwa Jina la Yesu tu ndipo wote tunapaswa kuokolewa nalo.
Baada ya mwaliko kwa Simoni mkoma Yesu aliingia Yerusalemu amepanda mwana punda na watu wakamshangilia "Hosana."

*Toa akili yako kwa ajili ya vitu vya kiroho. Epusha akili yako na kujitegemea mwenyewe. Panda roho ya kuridhika, yenye uchangamfu. Unazungumza sana juu ya vitu visivyo vya muhimu. Haupati nguvu ya kiroho kutoka katika hayo. Ikiwa nguvu ulizotumia katika kuongea zingetumika katika maombi, ungepokea nguvu za kiroho na ungemuimbia wimbo MUNGU moyoni mwako.
-------------------------------

Maswali: Kwa nini Wayahudi walitaka kumwua Lazaro aliyefufuliwa? Kayafa alitabiri nini? Siku kuu ya pasaka ilianzaje? Kwa nini Yesu alienda kukaa milima ya Efraimu? Kwa nini tunapaswa kumtii Mungu kuliko mwanadamu? Je unatambuaje kama mchungaji wako anakupitisha njia mbaya?

**SIKU YA 271.**
**(Septemba 27)**

# Wayunani wanamtafuta Yesu.

**Yohana 11 na 12.**



Palikuwa na hata Wayunani (kutoka Uyunani), walikwea siku ya sikukuu ya pasaka kule Yerusalemu pamoja na wengine ili kumwabudu Mungu wa Kweli wa Ibrahimu. Hawa walimwendea Filipo mwanafunzi wa Yesu wakamwomba "Bwana sisi tunakata kumwona Yesu." Walikuwa wamesikia habari za Masihi na kuamini japo walikuwa watu wa mataifa. Filipo aliendа kumwambia Andrea, naye andrea akamwambia Yesu Ambaye alikuwa anafundisha hekaluni. Ndipo wakamwuliza Yesu kama angependa kuwaona watu hawa; maana alikuwa ndani ya hekalu ambapo watu wa mataifa hawakuruhusiwa. Yesu akatoka nje kuzungumza nao kwa furaha. Yeye hakuwa na ubaguzi kwao, wote walikuwa watoto Wake. Wengi wa Wayahudi waliona wengine si wa muhimu, hata siku nyingine walisema Yesu aliendа kujificha kwa Wayunani, na wengine wakamwita Msamaria mwenye pepo. Wasijue japo walikuwa Wayahudi walikuwa wana mapepo mengi na Mungu waliyejivunia walikuwa wamemkataa. Yesu aliona watu ambao wamekubali kumpokea kama Mwokozi wao akawa tayari kuonana nao. Wayunani hawa walikuwa wanatoka miji ya Korintho, Athene, au Thesalonike. Walifurahi nao kumwona Yesu, Naye aliporudi kwa wanafunzi Wake alisema "saa imefika Mwana wa Adamu atukuzwe, amini amini

Nawaambia chembe ya ngano isipoanguka katika nchi au isipopandwa hubakia ile ile moja peke yake, bali ikifa ndiyo inazaa mbegu nyingi zaidi, na mavuno yanakuwa mengi."

Kama Yesu asingelikufa, basi matunda mema yasingekuwako. Kama mtu anaishi mwenyewe atapoteza ufalme wa Mungu bali kama akifa nafsi yake na akaishi kwa ajili ya wengine ndipo atatoa mazao mengi mema, na kupata uzima wa miele. Yeye ajipendaye nafsi yake ataiangamiza, na yeye aichukiaye nafsi yake ataisalimisha kwa uzima wa milele. Mtu akitaka kumtumikia Mungu lazima amfuate alipo na akiwa tayari kumtumikia Yesu, Baba wa mbinguni atamuheshimu. Akasema "nisemaje sasa roho Yangu imefadhaika, kwamba Baba nataka kujitoa katika kafara hii ninayoenda kuitoa? La! siwezi kusema vile, maana kwa ajili ya hiyo ndiyo Nilikuja duniani. Baba litukuze Jina Lako."

Hapo hapo ikatokea sauti toka mbinguni "Nimelitukuza, Nami Nitalitukuza tena." Kila mtu kwenye mkutano akasikia ile sauti ya Mungu Baba toka mbinguni kama ngurumo. Wengine wakasema "Malaika amesema Naye." Yesu akawambia sauti hiyo haikuwa kwa ajili Yangu bali kwa ajili yenu. Sauti ya Mungu ilikuwa imesikika mara tatu, wakati wa ubatizo, wakati wakiwa mlimani alipobadilika kwa mng'ao, na sasa katika hekalu. Wayunani walielewa kabisa ishara na Maneno yale BABA Alisema na wakaenda wamebarikiwa.

Akawaambia Shetani mkuu wa ulimwengu huu karibu atatupwa, wakati Yeye anapoenda kutuokoa sisi wanadamu kwa kifo Chake. Akawaambia kwamba "Nami nikiinuliwa juu ya nchi Nitawavuta wote Kwangu." Alikuwa akiwaonyesha jinsi atakavyokufa kifo cha msalaba na kuinuliwa ili kutuokoa. Yesu sumaku ya dunia ameinuliwa na watu toka kila taifa, lugha, jamaa, kabila, kutoka magharibi, kusini, kaskazi na mashariki wanamfuata. Watu wakamwambia wakisoma Maandiko walifikiri Masihi ataishi nao milele wala hatakufa. Akawaambia La! Na kuwaeleza kwamba Yeye ndiyo nuru, sasa wana nuru waenende katika matendo ya nuru na si giza, maana aliye gizani hajui aendako, akaawaambia kwamba "maadamu mna nuru, tembeeni nuruni mpate kuwa wana wa nuru." Maana nuru ni Neno la Mungu, na Yesu ni Neno la Mungu.

Walionyeshwa miujiza mingi, ila wengine hawakusadiki kama Isaya alivyosema "amewapofusha macho, ameifanya mizito mioyo yao; wasije wakaona kwa macho yao, wakafahamu kwa mioyo yao, wakaongoka nikawaponya." Ila wakuu wengi wanaomwamini waliogopa kumkiri wasije wakatengwa na sinagogi, walipenda utukufu wa wanadamu kuliko utukufu wa Mungu. Yesu akasema amwaminiye Yeye huamini Baba wa mbinguni aliyempeleka. Akasema amekuja kuokoa ulimwengu na wala siyo kuuhukumu. Yesu aliwapenda watu Wake katika ulimwengu kupita upeo, mpaka mwisho.

Mtoto usiwe na hofu, Yesu anarudi tena kutuchukua, anatupenda na ana furaha kurudi tena kutuchukua. Tusome Neno Lake tuliamini na tulitumaini. Wayunani au Wayunani wanatuwakilisha sisi sote wa mataifa tofauti leo; hebu tuseme 'tunataka kumwona Yesu'. Yesu aliona maono mpaka mwisho wa dunia ya wale wote

watakaompokea, akapata furaha kubwa ya kuukabili msalaba, akaipuuzia aibu ili wewe na mimi tuokoke.

*Baraka kuu ambayo MUNGU anaweza kumpa mwanadamu ni roho ya maombi ya dhati. Mbingu zote zimefunguliwa mbele ya mtu wa maombi. Mabalozi wa Kristo watakuwa na nguvu kwa watu baada ya wao, kwa sala ya dhati, kuja mbele za MUNGU.

--------------------------------

Maswali: Kwa nini Wayunani walimtafuta Filipo? Yesu alisemaje kuhusu Wayunani? Wayunani wanawakilisha nani leo? Sauti ya Mungu iliyosikika ilisemaje? Mwana wa Adamu kuinuliwa ina maana gani? Punje kuanguka na kufa ina maana gani? Je nawe wataka kumwona YESU leo?

**SIKU YA 272.**
**(Septemba 28)**

# Kualikwa arusini.

**Mathayo 22. Luka 16.**



Yesu akatoa mifano ya ufalme wa mbinguni, kuwa umefanana na mfalme mmoja aliyemfanyia mwanawe arusi. Akatuma watumwa wake wawaite watu mashuhuri walioalikwa arusini; akitegemea watakuja, nao wakakataa kuja. Akatuma tena watu kwa wengine, akisema waambieni wale walioalikwa, tazameni nimeandaa karamu yangu, ng'ombe nimechinja, na vinono vingine vingi vimekwisha kuandaliwa njooni arusini.

Akaweka nyimbo za kusikiliza, akingoja watu. Wale watu walioalikwa hawakujali, wakaenda zao, mmoja akatoa udhuru akisema hatakuja arusini ameoa mke, na mwingine akasema amenunua shamba, na mwingine amenunua jozi tano za ng'ombe yabidi ajaribishe, mwingine akasema anaenda kwa biashara yake. Basi wale watumishi wakatoa taarifa kwa bwana wao, kwamba wanaoalikwa hawana nafasi.

Wote hawakujali wakaendelea na yaliyo ya muhimu machoni pao. Wengine waliokataa kuja arusini waliwakamata watumwa walioalikwa na kuwafanyia ukatili hata kuwaua. Mfalme alighadhabika, akapeleka majeshi yake, akawaangamiza wauaji wake, akauteketeza mji wao. Kisha akawaambia watumwa wake arusi i tayari, ila walioalikwa hawakustahili. Basi enendeni hata njia panda za barabara, na vichochoro na wote muwaonao, wawe masikini vilema, viwete au vipofu waiteni arusini.

Watumwa wale wakatoka na kwenda njia kuu, wakawakusanya wote waliowaona, waovu na wema. Arusi ikajaa wageni masikini, na watu wa kawaida, hakuna tajiri au wafalme waliokuwamo bali watu wanaozurura barabarani tu. Hawa walikuwa hawajavaa nguo nzuri, bali walikuwa na furaha na shukurani mioyoni mwao.

Watumishi wakajitahidi wajaze watu mle toka kila mahali. Wakakazana kuwaalika watu tena na tena.

Mungu anaonyesha upendo Wake mkuu kwa dunia hii, amechukua muda kutayarisha vyote vitakavyotupa furaha, na anataka tushiriki pamoja, ila watu wengine wana 'shughuli' nyingi, wanatoa udhuru, mmoja baada ya mwingine. Udhuru hata usiokuwa na mkia wala mguu. Tuwe na tahadhari, Mungu ametualika kwenye karamu Yake tusitoe udhuru, mara siendi kanisani leo, nataka kucheza mpira, na wenzangu, au sina suti ya kuvaa.

Wengine husema sina haja ya kwenda kanisani leo, naangalia programu ya runinga. Wengine husema nimechoka wacha nilale, sitaki kupiga magoti na kuomba leo au bora nisome vitabu vya tamthiliya au hekaya badala ya kusoma Neno la Mungu. Wengine wanatoa udhuru kuhudumia watu, siwezi kumsaidia ana donda ndugu, au ananuka, au nahitaji nijipinde mno na kukosa raha nikitembelea watu gerezani. Kuna kila aina za udhuru, binadamu wote hutoa ili wasifanye yale Mungu anataka wafanye. Cha kugundua ni kwamba udhuru mwingine haukubaliki na Yesu, maana ni kama kusema "sijali kufanya jema au baya, nataka kufanya ninachotaka." Viudhuru vingine ni vya hatari, kwa vile vitatufanya tusiwe zizini mwa BWANA leo; na kisha vitatuelekeza kwenye visababu vingine, na mwishowe, vitatufanya tusiingie mbinguni.

Wale walioalikwa hakuna hata mmoja aliingia karamuni isipokuwa wale wa dharura. Mtu huyu mwenye karamu alisikitika kwamba hawakuja. Lakini alipoingia yule mfalme mwema, kuwatazama wageni wake, aliona karamuni, mtu mmoja asiyevaa vazi la arusi. Kukawa na kimya, maana aliwapa kila mmoja vazi la kuvaa kwenye arusi hii, basi akamwuliza yule mtu "ndugu, uliingiaje humu bila vazi la arusi?" Yule mtu kwa woga, akanyamaza, ndipo kila mtu aliposhangaa mfalme alipotoa amri, yule mtu afungwe miguu na mikono na kutupwa nje. Huu ndiyo ulikuwa mfano wa arusi, mfano wa mwisho kati ya ile mifano kama 29 iliyorekodiwa. Je, maana yake ilikuwa nini? Mungu Ndiye Mfalme Yule aliyefanya harusi ya Mwana Wake Yesu, na kuita viongozi wa Israeli, na watu wote.

Watumwa wa Yule mfalme ni manabii na watenda kazi wa Mungu, ambao amewatuma wawaambie mara nyingi viongozi hawa watubu, na kurudi Kwake. Watu waliokuwa barabarani wale masikini, na wahitaji, wazuri na wabaya, walikuwa wavulana, wasichana, wanaume na wanawake waliokuwa wanamsikiliza Yesu, na ni ombi letu hao wanatuwakilisha sisi. Aliwaambia hili kwa vile alitaka wajitayarishe, aliwaonyesha na wakajua wanakaribishwa kwa BABA Yake. Hata wakiwa masikini, wasioenda shule, wenye nyumba duni, au wasio na baba, mama au wazazi wote, au chochote ambacho chaonekana kizuri au cha maana mbele za watu; kinachojalisha ni wanakubali mwaliko wa upendo wa Mungu ili washiriki yote mazuri ambayo anayo.

Karamu ya arusi ya Mfalme wa mbinguni, iko wazi kwako na kwangu leo. Kuna sharti moja tu, nalo ni tuwe na vazi la arusi, liwe safi, na zuri. Je, vazi hili nini? Ni usafi wa moyo, utu wema, na moyo unaosamehe kama wa Yesu. Ni vazi la haki ya

Kristo, vazi hili la utukufu Wake, lazima livaliwe na kila mtu anayehudhuria arusi. Yeye analitoa kwetu sisi, tulikubali, nasi tulivae . Maana binadamu hana vazi la haki, au vazi la kufaa. Kila tunapopewa mwaliko na watu wa Mungu leo, ni sauti ya Mungu, tusiipuuzie, maana tukipuuzia sauti itakuwa dhaifu, na ndogo zaidi mpaka mioyo yetu itazoea dhambi, kisha siku moja tutapoteza wokovu.

Tutapoteza wokovu, si kwa sababu tulikuwa waovu, La hasha, bali kwa sababu tumepuuzia nafasi tulizopewa kuikubali ile Kweli. Mungu hataokoa watu wanaoonekana 'wazuri', bali watu wanyenyekevu, wanaomjua Yeye, wanaomtumiani, na kumtegemea, wakijisalimisha Kwake asilimia mia moja.

Tuchukue tahadhari tusimwangushe Mungu wetu, anapotualika karamuni Mwake. Karamu hii ni mbingu. Yesu atakuja kutuchukua, twende Naye, itakuwa huzuni na aibu, endapo marafiki zetu, au mambo ya dunia yatafanya tukose karamu hiyo. Jenga urafiki na watu watakaokusaidia kwenda kwenye hiyo karamu, na uweke makini kusaidia wengi wahudhurie hiyo karamu, ndiyo itafanya maisha yako yawe na sababu.


*Maombi Huleta Nguvu Kutoka kwa MUNGU- Nguvu zitatoka kwa MUNGU kwenda kwa mwanadamu kujibu maombi ya imani.
----------------------------

Maswali: Je twawezaje kwa maisha ya leo kupuuza mwaliko? Mfalme aliyefanya arusi ni nani? Jadili "Sisi ni bibi arusi tunamngoja Yesu aje." Vazi la arusi ni nini? Je, tunajuaje kwamba tumepuuzia mwaliko, ili tufanye hima na kuukubali mwaliko?

**SIKU YA 273.**
**(Septemba 29)**

# Mwanakondoo aliyepotea, sarafu iliyopotea.

**Luka 14.**



Yesu akasema mtu akija Kwake na hamchukii baba, mama, mke, mwanawe au ndugu zake wa kiume na kike na hata nafsi yake mwenyewe, huyo hamstahili Yeye kuwa mwanafunzi Wake. Mtu yoyote asiyeuchukua msalaba wake na kumfuata Yesu nyuma, hawezi kuwa mwanafunzi Wake. Maana ni nani akitaka kujenga mnara asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kwamba anavyo vya kuumalizia? Asije akashindwa uumaliza baada ya kuupiga msingi, watu wote wataanza kumcheka na kumdhihaki, wakisema mtu huyu alianza kujenga; akaishiwa pesa na kukosa nguvu za kumaliza.

Au kuna mfalme gani ambaye anaenda kupigana na taifa jingine asiyeketi kwanza na kufanya shauri na watu wanaohusika na uchumi na jeshi ili aone kama yeye pamoja na watu 10,000 waweza kukutana na lile Jeshi la adui na kulishinda? Na kama akiona hawezi, hutuma ujumbe kutaka amani na lile Jeshi la adui ili asiumizwe, akali mbali. Hali kadhalika kila mmoja asiyeacha vyote alivyo navyo hawezi kuwa mwanafunzi Wangu, akasema Yesu “kila aliye na masikio asikie.”

Watu wakamnung’unikia kwamba anakula na wenye dhambi na watoza ushuru. Ndipo Akawapa mfano akisema, Ni nani kati yenu mwenye kondoo mia akapotelewa na mmoja, asiyewaacha wale 99 ili aweze kumfuatia yule mmoja nyikani. Ataenda amtafute mpaka amwone yule mmoja, naye akiisha kumwona, humweka mabegani pake akifurahi. Wala hamgombezi! Naye akifika nyumbani huwaita marafiki zake na kuwaambia furahini, pamoja nami, kwa kuwa nimekwisha kumpata mwanakondoo wangu aliyepotea. Yesu akasema, vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye kuliko kwa ajili ya wenye haki 99 ambao hawana haja ya kutubu au wapo zizini tayari.

Kila mtu pale alielewa ule mfano, maana wangefanya vile kwa mifugo yao, au

walikuwa wameshafanya vile tayari. Kondoo aliyepotea kwa mfugaji ni kitu cha thamani. Na wafugaji wanaelewa hii lugha, wanapiga mbiu na kuwaomba watu wasaidie msako hata iwe usiku! Wengi waliofuga wanyama hawa waliwapenda na kuwajua kwa majina yao. Walitafuta malisho na maji kwao. Walitambua ni wakati gani Kondoo anapokuwa na shida, furaha au huzuni. Walitembea umbali mkubwa kuwatafuta kondoo wao wakipotea. Walihatarisha maisha yao kwa wanyama wakali, walitembea kwenye mvua, barafu na hata vimbunga.

Walipanda milima na kwenda mabondeni, na hata kuwaambia majirani wawasaidie, walipoona mifugo ina shida. Mifugo mingine ilipendwa kama watoto wa nyumbani. Basi mvulana yoyote au msichana ana thamani ya pekee kwa Mungu wake. Hakuna kama wewe, Kwa Mungu una thamani zaidi ya kondoo aliyepotea. Umeumbwa kwa mfano wa sura ya Mungu. Kuna furaha kuu mbinguni, unapoomba msamaha unapokosea, kuliko wale walio sahihi, ambao hawahitaji msamaha. Mungu anakujua kwa jina lako, na anafanya juu chini upate uzima wa milele.

Yesu alizungumza upendo wa Mungu na utayari alio nao kusamehe. Hata wale waliofanya uovu mkubwa walipata faraja, watu waovu wengi walikuja wamsikilize, wengine walikuwa wezi, walaghai, waongo, wenye wivu, wasengenyaji na wale wanaochukuwa wake au waume za watu wengine. Ndani ya mioyo yao watu hawa walitaka kuishi maisha bora kwa kubadilisha maisha ya zamani, ila hawakujua wafanyeje. Walifikiri haiwezekani baada ya kutumbukia uovuni, kurudi katika njia njema tena, mpaka Yesu alipowafikia.

Wakajazana, kumsikiliza, mioyo yao ikaburudika, na kupata faraja. Ila mafarisayo, makuhani na waandishi wa sheria waliona ni ajabu, wakififikiri wao ni wakamilifu waling'aka "mtu gani huyu anayepokea waovu wenye dhambi na kula nao." Wakamng'ong'a, wakambeza na kumsonya. Hawakujua waliyokuwa wakimsema Yesu kwa nia ya kutaka yampe sifa mbaya yalimpa sifa nzuri, na kuilenga tabia Yake kwa namna ambayo watu wengi waliweka usikivu "kwa kuwa mwana wa Adamu alikuja kuokoa kilichopotea, na kumpa kila mtu matumaini."

Akasema kuna mwanamke gani mwenye sarafu kumi za fedha ambaye akipotewa na moja asiyewasha taa na kufagia nyumba, na kutafuta kwa bidii hata aione? Ataacha shughuli zake zote alizo nazo, iwe ni kufua nguo, kuchota maji, kupiga deki, kupika chakula au kusenya kuni; na kuweka nguvu zote kwenye kuitafuta hii sarafu. Kwa vile kuna giza, na madirisha ni madogo au sakafu ni ya udongo, atatumia muda na kutia uzito. Na akiisha kuiona atawaita rafiki zake na jirani zake akawaambia kwa tabasamu, furahini pamoja nami kwa kuwa nimeipata tena shilingi ile iliyonipotea. "Nawaambia vivyo hivyo kuna furaha mbele ya Malaika wa Mungu kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye."

Mifano hii miwili inatofautiana kidogo ikionyesha kuna watu waliopotea kama mwana-kondoo ambao wamejua wamepotea ila hawafahamu warudije. Hawa inabidi tuwasaidie kama ndugu katika BWANA. Kuna wengine hawajui wamepotea na hivyo hawana habari kama inabidi warudi kama ile sarafu. Kisha Yesu alitoa kisa cha mwana mpotevu, aliyejua amepotea na alijua njia ya kurudi kwa babaye.

Ezekieli 34, Yasema leo sisi tu wachungaji wa ndugu zetu, ila mara zingine wachungaji wanafanya makosa. "Ole wao wachungaji wa Israeli wanaojilisha wenyewe, Je haiwapasi wachungaji kuwalisha kondoo? Mnawala walionona; mnajivika manyoya, lakini hamwalishi kondoo. Wagonjwa hamkuwatia nguvu, wala hamkuwaponya wenye maradhi, wala hamkuwafunga waliovunjika wala hamkuwarudisha waliofukuzwa, wala hamkuwatafuta waliopotea; bali kwa nguvu na kwa ukali mmewatawala, nao watatawanyika kwa sababu hapakuwa na mchungaji; wakawa chakula cha wanyama mwitu. Walitangatanga, hakuna aliyewaulizia, wala kuwatafuta." Malisho ni Neno la Mungu la uzima. Yeyote yule anayeleta mapokeo na mafundisho ya uongo, nje ya Maandiko, ni mwizi wa kondoo za Yesu. Yesu atatuongoza leo mahali kondoo waliopotea walipo, nasi tuwarudishe kwa upendo, na siku nyingine nasi tukipotea, wengine watatusaidia kurudi ili tusiangamie na wanyama mwitu. Mtumishi wa Mungu asijali kula mali za kondoo, kuliko kuwalisha Neno la uzima.

Basi Yesu akajulikana kama rafiki wa wenye dhambi, alikaa nao na kuwapa matumaini, hata wale wenye uovu kiasi gani, wabaya kupita wote, waliotoka kundini wakaenda mbali sana, walijua sasa kwamba kuna mtu anawajali. Malaika wa mbinguni wakafurahi mno, maana aliwahakikishia kwamba "kuna furaha mbinguni kwa mwenye dhambi mmoja tu, akiungama na kurudi tena zizini." Upendo ni sumaku kubwa, upendo wa Yesu ulivuta mioyo ya wengi, na kuwakwamua kutoka kwenye minyororo ya Shetani, na kuwaleta kwa Mwenyezi Mungu.

Yesu alijua watu watamcheka, watamtemea mate, watamzomea, watamtesa, watampiga mijeledi, na watamwua ila hakurudi nyuma. Katika pambano lile kuu tulilo nalo lililoanzia mbinguni na uasi wa Shetani, linasukuma binadamu wafanye uovu. Binadamu lazima aelewe adui yake ni Shetani kila kukicha, na si mwanadamu mwenzake au Mungu, na kisha avae silaha za Mungu za Waefeso sita. Maana watu hawa waliponywa na Yesu na walitatuliwa shida zao zote. Kila alikopita hakusalia mgonjwa hata mmoja. Hawakuhitaji hospitali, operesheni, pesa au kulazwa bali hata hivyo walimwua. Hivi leo tungekuwa na mtu kama huyu miongoni mwetu na mtu amwue, si tungefikiria ni mwehu? Basi ndilo pambano kati ya wema na ubaya lilivyo, uovu hauna sababu ya kutokea, ungekuwa na sababu ungekoma kuwepo.

*Maombi Yanayoishikilia Nguvu isiyo na Ukomo - Imani ya Kweli na ombi la Kweli — ina nguvu kiasi gani! Ni kama mikono miwili ambayo mwombaji wa kibinadamu hutegemea na kushikilia nguvu ya Upendo usio na mwisho.

--------------------------

Maswali: Mwanakondoo aliyepotea anamwakilisha nani? Mchungaji mwema ana sifa gani? Walipolalamika Yesu anakula na wenye dhambi alitoa mfano gani? Kwa nini wachungaji wa Israeli walipewa ole? Mwanamke mwenye sarafu kumi anafananishwa na nani? Kwa nini Yesu hakurudi nyuma kutupenda?

**SIKU YA 274.**
**(Septemba 30)**

# Mwana mpotevu au mtoto aliyekimbia kwao.

**Luka 15**



Katika mifano ya ajabu aliyotoa Yesu, mfano huu ni mojawapo kati ya iliyogusa mioyo mno. Akatoa mfano wa mtu mmoja aliyekuwa na wana wawili. Mkubwa mtu wa bidii ya kazi na anawajibika akitumwa. Yule mdogo, alikuwa mvivu, mponda mali, na mpenda anasa; huyu akamwambia babaye, "Baba nipe sehemu ya mali yangu." Hili lillikuwa jambo zito, maana kuomba urithi kabla baba hajafa ilikuwa ni kutaka baba yake afe. Mwana huyu alitaka awe huru, akivinjari sehemu za mbali duniani, ili afiche dhambi yake mbele ya babaye maana alijua kanuni za baba yake, akaona woga kufanya zile dhambi mbele ya macho yake na mbele ya jumuiya aliyoishi.

Basi yule baba akagawa sehemu ya urithi wa yule kijana na kumpa, na baada ya siku nyingi yule kijana mdogo alikusanya vitu vyake na kusafiri nchi ya mbali, wengine wanaita majuu, naye akatapanya mali yake kwa kufuja huko kwa maisha ya uasherati na anasa. Alifurahia na hili zoezi, akitalii kila mahali penye vitu vya kutamanisha macho, akala vyakula vya kila namna.

Hakuwa na uchungu na pesa kwani hakuzitolea jasho, zilikuwa za urithi! Watu wakampokea kila mahali maana walijua wataponda mali yake pamoja naye; ni rahisi kuwa na marafiki ukiwa na pesa au siku ya kulipwa mshahara 'urafiki wa mwisho wa mwezi'. Akawanunulia marafiki zake vitu kama pombe, na akaendelea kuishi maisha ya gharama. Pesa ikazidi kupunguka, mpaka ikaisha, asipate wa kumshauri, au waliomshauri aliwaapuuzia kwamba ni masikini hawajui kitu.

Alipokuwa amekwisha kutumia kila senti, marafiki walihama na njaa kuu iliingia nchi ile chakula kikapungua, nguo zilitoboka, yeye naye akawa amefilisika na kuwa mhitaji, na akaenda kwa mwenyeji kutafuta kibarua. Akapelekwa shambani na mwajiri kulisha nguruwe; mate yakamtoka akitamani kujishibisha kwa maganda waliyokula nguruwe, wala hapana mtu aliyempa kitu, akasikia kizunguzungu kwa njaa.

Alipozinduka na kufikiri moyoni mwake, alijiuliza hivi "watumishi wa baba yangu wangapi walioko? Wanakula na kusaza na mimi natabika hapa nakufa na njaa, na kufanya kazi ya kutunza nguruwe wachafu hapa, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba nimekosa juu ya mbingu na mbele yako. Sistahili kuitwa mwana wako, tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako." Uvivu ukamtoka, maana hakuna alichopewa bure bila kufanya kazi.

Akajua dhambi aliyoifanya ya kutomjali Mungu na mapenzi Yake kwake. Hakujali kama anamwumiza moyo wa babaye, bali alijifikiria yeye tu. Akatamani kwao, akaona ukiwa, hakuna aliyemjua au kumthamini ugenini, walimpenda kwa pesa zake tu. Kisa hiki cha huzuni, Yesu alikitoa ili vijana wasijisahau, kufikiri dunia ina vitu vyema kwao, kwani wataingia kwenye hasara za maisha yao ya kimwili na kiroho. Kijana akisha kupanga hotuba au ngonjera yake kwa baba, akawa tayari kuomba msahama wa dhati. Aligundua uasi wake, na akawa tayari aishi kama mjakazi, na hakupoteza muda. Baba alijua kijana ameuteketeza urithi bali alimpenda.

Kijana akaondoka na kwenda kwa babaye, alikuwa na njaa, akatembea pole pole, akifikiri atakavyopokelewa nyumbani pengine hawatamkubali tena. Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, alikuwa kila siku akikaa juu kilimani akiangalia kwamba kuna siku mwana wangu mpendwa atazinduka na kujua amefanya kosa na kuja tuishi pamoja kwa furaha tena. Basi baba yake alipomwona alimwonea huruma, akaenda mbio kwa mwanawe, naye kijana akawaza ni nani huyu anayenijia? Babaye alienda akamwangukia shingoni akambusu sana.

Hakumbusu kidogo, japo alikuwa na nguo chafu, na harufu za nguruwe. Yule kijana mdogo alianza kuirudia ile risala aliyokariri, akaanza kuirudia "Baba nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena." Ila baba hakutaka kusikiliza, wala hakuacha amalizie risala hiyo; bali aliwaambia watumwa 'Leteni upesi vazi lililo bora, mkamvike mtieni na pete kidoleni na viatu vipya miguuni, mleteni ndama mnono na mumchinje na tupike na kufanya karamu kubwa na kufurahi. Kwa kuwa mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka, alikuwa amepotea naye ameonekana."

Kijana akafurahi, hakuwa ametegemea atakaribishwa vile, alikuwa tayari kuishi zizini, sasa amepewa chumba kizuri alichokuwa analala kabla ya kuumiza moyo wa babaye, na amepewa mavazi, viatu na hata pete ya familia. Pete ya familia inawakilisha kumiliki au kuwa mtawala. Akaenda kuoga atoe harufu ya nguruwe mwilini, Watu wakaanza kushangilia na makelele yalisikika kwa mbali wageni walioalikwa kwa karamu wakiwasili.

Baba akarudia kwa furaha kusema "Eh mwanangu! Jamani nilifikiri kafa, kumbe yupo, Mungu mkuu." Ndivyo alivyo BABA wa mbinguni, haijalishi tumefanya uovu wa namna gani na kugeuza nyuso zetu mbali Naye, tukirudi Yeye Yu tayari kutupokea, ni Mwenye upendo, huruma na rehema, za milele. Anajua tunajipenda, na tutajiumiza bali tukirudi Anatupokea. Kuwa mwana mpotevu si lazima mtu aende nchi ya mbali.

Mtu aweza kuwa mwana mpotevu akiwa kanisani au nyumbani kama kaka wa mwana mpotevu. Mwana mpotevu alifikiri atapata anayostahili, ila Baba alisema nitakupa unachohitaji na si unachostahili. Tunachohitaji toka kwa Mungu ni neema na rehema. Tunachostahili ni kifo. Baba hakutaka kubania au kufanyia ubahili vitu, bali alitaka kufanya sherehe kubwa. Mungu anapenda sherehe! (GOD loves partying)

Akaja kaka mkubwa toka shamba akiwa amechoka. Alikuwa anasaidia kazi za nyumbani kama kutoa mavi ya farasi zizini na kazi hiyo aliifanya toka yule mdogo amepotea na kwenda kuponda mali. Huyu naye alitaka kuponda mali au kufanya sherehe ila alikuwa anashika sheria tu kumridhisha baba ila hakuwa na upendo. Alikuwa ana matendo mema, ila ndani ya moyo wake alikuwa hajaongoka. Kutenda matendo mema kama Mfarisayo na kuwa mwema ni vitu tofauti. Huyu ni kama muumini aliyekuwa akienda kanisani tu si kwa kupenda ilimradi amridhishe baba ila moyo ulikuwa hauna upendo kwa baba.

Huyu akasikia sauti za nyimbo na michezo, akamwita mtumishi mmoja na kumwuliza, ni nini kinaendelea hapa? Naye akajibiwa "Salalee! hujapata habari? Ndugu yako amekuja, na baba yako amechinja ndama aliyenona, kwa sababu amempata tena, yu hai na mzima." Kaka mkubwa akakasirika sana maana huyu bwana mdogo ameponda urithi wake na sasa ataka kuja kumaliza sehemu yake pia. Kuna nini afurahie na huyu 'ni heri bwana mdogo akae na njaa na uhali maana analipwa uovu wake'.

Akakataa kuingia ndani akizira au kuweka mgomo. Akawaza yule mdogo wake, mvivu na mjinga amerudi na kupokelewa kwa makeke na shangwe kana kwamba ni mfalme? Babaye akatoka nje ajaribu kumpooza moyo na akamsihi aingie, akakataa na kumjibu babaye "Tazama mimi nimekutumikia miaka mingapi hii? Wala sijakosa amri yako wakati wowote lakini hujanipa hata mwana mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu. Lakini alipokuja huyu mwana wako mponda mali yako pamoja na makahaba, umemchinjia yeye ndama aliyenona na kumpokea kama vile hukumbuki alivyokufanyia."

Mwana mkubwa akafikiri yeye amejitoa mhanga kumsaidia baba, bali baba hajawahi kumwuliza hata njozi au kile anachopenda amfanyie. Baba akasema akijaribu kumpoza kijana mkubwa akisema “mwanangu, wewe u pamoja nami siku zote, na vyote nilivyo navyo ni vyako, maana ndugu yako alishachukua sehemu yake. Imetupasa furaha na shangwe, maana alikuwa amekufa naye amefufuka, alikuwa amepotea naye ameonekana naye pia ni mwanangu huyu.”

Kijana mkubwa hakumjua baba, yeye ndiye alikuwa mwenye mali zote sasa, bali alikaa na baba kama mtumishi, asijue baba anampenda sana. Yeye alifikiri baba anampenda kwa kutunza amri, naye akajitahidi kuzitunza hivyo hivyo maana hakuwa na jinsi. Baba akamwambia hamna shida kila kitu ni chake, na maisha ni zaidi ya kufanya kazi ngumu. Akamshukuru kwamba “nakushukuru kwa kuwa mhimili wa nyumba wakati huu wote, ila nataka uwe na furaha tena, na kujua kwamba kumpenda mdogo wako hakuna maana nakuchukia wewe, au nitampa haki yako, La! hasha, maana huyu pia ni mwanangu Mimi.”

Wako hata leo watu wa namna hii wakiona mtu anarudi kwa BWANA wanakasirika badala ya kufurahi kama vile wanapungukiwa na kitu fulani, kumbe wanaongezewa mengi, maana mtoaji ni Mungu, Naye anaona huduma zao za upendo. Basi wao wasianze kunung’unika. Hata hivyo hakuna binadamu ambaye hajawahi kuwa mwana mpotevu. Hakika sijawahi kukutana na mtu wa namna hiyo! Basi kaka mkubwa akawa naye kama mwana mpotevu kwa ajili ya kukosa upendo, asitake kusahau ya zamani amfurahie kakaye kwamba amerudi nyumbani.

Hata leo wengine wakiona mtu aliyekuwa mwovu, mlevi na mharibifu anaachana na uovu wa zamani wanaona wivu kwamba pengine atafanikiwa na atawapita, au hawapendi naye awe bora na afike mbinguni wanataka wao tu ndiyo wapate zawadi au neema hiyo. Baba huyu kwenye kisa ni mfano wa Mungu. Ana furaha mpotevu anaporudi Kwake, haijalishi ameishi maisha ya kujichafua kiasi gani, anapoungama kwa toba ya dhati anakaribishwa tena. Mungu ni upendo hebu tuwe na shukurani za dhati Kwake na kumpenda Yeye na binadamu wote.

Yesu aliona makuhani na mafarisayo wana wivu wa namna ile, Yesu alipomponya mgonjwa, walijaribu kuzima furaha yake. Hebu turuke ruke kwa shangwe na kupiga vigelele, kwamba tunaye BABA anayetupenda.

*Wale ambao hawataki kuacha kila dhambi na kutafuta kwa bidii baraka ya MUNGU, hawataipata. Lakini wote watakaoshika ahadi za MUNGU kama alivyofanya Yakobo, na kuwa na bidii, unyofu, na uvumilivu kama yeye, watafaulu kama alivyofaulu.

-------------------------

Maswali: Mwana mpotevu alimwomba nini babaye? Kwa nini Mwana mpotevu alirudi nyumbani? Baba wa mwana mpotevu anamwakilishaje Mungu? Matendo yetu yanafananaje na ya Mwana mpotevu? Yule kaka mkubwa naye pia alikuwa amepotea kwa jinsi gani? Je, unafikiri kaka mkubwa naye aliungama?

**SIKU YA 275**
**(Oktoba 1)**

# BWANA aosha miguu.

**Mathayo 26 Yohana 13.**



Ikawa Yesu alipomaliza mazunguzo na wanafunzi Wake, aliwaambia "Mwana wa Adamu anaenda kusulibiwa." Wakati ule wakuu wa makuhani walikusanya wazee, waandishi na mafarisayo kuamua jinsi watakavyomkamata Yesu na kumwua, ila walisema isiwe wakati wa sikukuu ya pasaka, isije watu wakaleta ghasia nasi tusifanikiwe lengo letu. Hata siku ya kwanza ya juma la pasaka, inayoanza alhamisi jioni, wanafunzi Wake wakamwendea wakamwambia "Ni wapi utakapo tukuandalie pasaka?" Akawaambia waende mjini, na hapo watamwona mwanamume fulani, amebeba mtungi wamfuate na kumwambia "Mwalimu asema majira Yangu ni karibu; kwako nitafanya pasaka pamoja na wanafunzi Wangu, nitengee chumba kimoja kikubwa ghorofani kwa ajili ya mlo huo." Sikukuu ya pasaka ilianza wana wa Israeli walipotoka utumwani. Waliagizwa kuchinja mwanakondoo na kuweka damu yake kwenye kizingiti cha mlango, ili malaika apitapo kuua wana wa kwanza wa Wamisri, apite milango yao bila kuwadhuru.

Pasaka ilionyesha Mungu ni mkombozi wa kuwatoa kwenye utumwa wa Misri na zaidi utumwa wa dhambi. Damu ile ya kupaka kwenye kizingiti cha mlango iliwakilisha au ulikuwa mfano wa damu ya Yesu ambayo ingemwagika msalabani, ambayo Ndiyo ondoleo la kweli la dhambi. Damu ya wanakondoo isingesaidia wokovu, ni Mwana-Kondoo tu wa Mungu aliyeweza na anayestahili kuwakomboa wanadamu. Damu ya mwanakondoo, ilitumika kuwaelewesha wana wa Israeli kuwa Yesu Ndiye Ambaye anatutoa kwenye utumwa wa dhambi. Wanakondoo waliochinjwa walikuwa ni kivuli tu na Yesu ndiyo kafara halisi kwa ulimwengu wote. Wanafunzi walifanya kama walivyoagizwa na wakaiandaa pasaka. Wanafunzi walikuwa bado wanaoneana wivu, wabinafsi, na wenye viburi. Hawakung'amua kinachoendelea japo Yesu aliwaambia tena na tena kuwa anaenda kufa. Yesu alitaka kuwaambia mengi, ila hawakuwa tayari. Alipofufuka na kupaa, wakifanya kazi kubwa na kwa bidii huku wakitamani siku zile walizokuwa na Yesu wangezitumia kumwuliza maswali yanayowatatiza. Hata leo nasi tusipoteze muda mara tusikiapo Neno la Mungu. Yesu katika mlo huu aliwaonyesha kuwa kinachomfanya mtu kuwa mkuu ni upendo wake na huduma yake kwa watu.

Yesu aliingia karamuni akijua Baba Yake amempa vyote mikononi Mwake, na Ibilisi amekwisha mwingia Yuda, aliondoka kando na akayavua mavazi yake kando, akatwaa kitambaa cha kuwaosha miguu na kujifunga kiunoni. Kisha akatia maji kwenye beseni na kuanza kuwatawadha miguu kama kawaida ya mtumwa kufanya kwa watu wakiingia nyumbani, maana hakukuwa na mwanafunzi aliyejitolea kufanya kazi hii. Pengine wengine walifikiri Yohana ndiye awasafishe maana ni mdogo wa wote, naye Yohana akafikiri mimi ndiye napendwa sana, wengine wafanye kazi hiyo ya kitumwa. Yohana na Yuda msaliti wakawahi wakae kushoto na kulia kwa Yesu.

Wengi tumeona hili kwa kukimbilia kukaa dirishani tukisafiri kwa gari ili tuwe na mawasiliano ya karibu na walio nje au kuona na kuzungumza na walio nje. Yesu Aliwafuta miguu yao baada ya kuwaosha na kile kitambaa alichojifunga. Alipofika kwa Simoni Petro, Petro alisema "Wewe wanitawadha miguu mimi? Na Wewe ni BWANA wangu na mimi ndiye mdogo?" Ila Yesu alimwambia asibishe bali akubali maana "Nifanyalo wewe hujui sasa lakini utalifahamu baadaye." Petro akabisha akiona haifai kwa BWANA kujishusha kwa kiwango kile akasema "Wewe hutanitawadha miguu kamwe." Yesu akamwambia asipokubali kutawazwa miguu basi hawezi kuwa mwanafunzi Wake.

Ilibidi Petro aonyeshe unyenyekevu na utii na akasema "si miguu yangu tu, bali hata kichwa na mikono yangu pia." Yesu akamwambia yeye aliyeoga hahitaji hayo yote bali miguu tu, ambayo ina vumbi baada ya kutembea, maana mwili wote u safi. Akasema wamekuwa safi maana wamezaliwa mara ya pili, wote ila mmoja Yuda msaliti. Yesu alipomaliza kuwasafisha miguu aliyatwaa mavazi Yake na kuketi tena akawaambia "mmeelewa kile nilichowafanyia?" Akasema "nyinyi mnaniita Mwalimu na BWANA, mko sawa maana ndiyo Ukweli wote.

Kama Mimi BWANA, nimewapa Mfano kwamba Nipo tayari kuwaosha miguu yenu, imewapasa nanyi pia kuoshana miguu hivyo hivyo, kwa kuwa nimewapa

kielelezo cha kuwa watumishi mnaohudumia watu na kuwajali; ili kama mimi nilivyowatendea nanyi mtendeane vivyo. “Amini mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka.” Mkiyajua hayo basi ni heri mkiyatenda, isiwe tu ni kujua bali mnajiweka juu ya kila mtu mkitaka kutumikiwa na kupata vitu vizuri wakati wengine wanateseka na kuhangaika. Ni kawaida ya binadamu wote kutaka kutumikiwa na kujiweka mbele ya wengine, au kutafuta faida kwa jasho la wengine. Unyenyekevu na kuhudumia watu, ni kitu tunachojifunza kwa Yesu. Hakipo kwenye asili yetu. Roho Mtakatifu Ndiye anayetusaidia kuwa tayari kwa huduma hii. Anatusaidia tujihoji, na kutoka pale kwenda kuhudumia wengine. Je unaweza kusema vile ambayo ungehudumia majirani zako?

Yesu alitoa Amri waumini waoshane miguu kabla ya pasaka, kama ukumbusho. Kuosha miguu baada ya kutembea na kupata mavumbi ni aina ya ubatizo mdogo. Ila mtu akitoka nje ya Mafundisho ya Kristo au kuasi, basi yabidi abatizwe. Ubatizo ‘mdogo au mkubwa’ ni kufanya upya nadhiri zetu tena, kwa utumishi kwa dunia na kwa waumini wenzetu makanisani kama mitume walivyofanya. Makanisa mengi yanatoa mafundisho kwa watoto ili waelewe, kabla ya kushiriki Komunio, yaani meza ya Bwana. Komunio si kitu cha kula tu ili mtu ashibe. Bali ni jambo la wakfu na takatifu. Pia ni wakati wa kuomba msamaha kwa Mungu na watu, kisha kusali na kuimba pamoja kwa wanaooshana miguu na kula pamoja. Kuoshana miguu ni huduma ya unyenyekevu, na uponyaji kwa waliokoseana.

Mkate na divai ni ukumbusho wa mwili na damu ya Yesu iliyotolewa kafara kwa dhambi zetu. Damu iliyomwagika kwa ajili ya dhambi zetu. Ni muhimu watu kujihoji na kutubu dhambi kabla ya kula pasaka au meza ya BWANA maana ni aina ya ubatizo au sakramenti, na si kama chakula chochote kile. Tunahuishwa kuanza maisha mapya tena kwa kula mwili Wake yaani kuingiza Neno Lake kwenye mioyo yetu. Watu wanapaswa kula na kushiba majumbani mwao kabla hawajaja kwenye huduma hii. Tusipokuwa safi na kisha tukala pasaka tunajihukumu nafsi zetu wenyewe. Hata hivyo hatujapewa mamlaka kuwahukumu wengine.

Waumini wote wanaruhusiwa kushiriki katika huduma hii. Huduma ya kuosha miguu iliwapa mitume kielelezo cha kutokuwa na ubinafsi wa kujifikiria na kujitumikia wao wenyewe. Yaani ni huduma inayolenga kukuza unyenyekevu. Yesu aliosha miguu ya wale waliokuwa tayari kumkana na hata kumsaliti bila kuwaumbua. Leo wengi wakisikia mtu anamvizia au kumfanyia ubaya, watatangaza kwa wengine au kufanya mipango fulani ya kulipiza mabaya wanayofanyiwa wao. Mungu haishi kwa ajili Yake Mwenyewe, bali anaishi kwa ajili yetu sisi viumbe Vyake. Hata leo sisi sote tumeoshwa dhambi zetu zote na Yesu. Iwe ni hasira, uongo, wivu, au kiburi vyote vimeoshwa. Tendo la unyenyekevu alilolited a Yesu la kuoshana miguu linatufundisha kuwa sisi nasi twapasa kufanya hivyo leo.

Yesu akasema amewaambia yote haya, hata yale ya Yuda Iskariote ambaye “atamwinulia kisigino kwa kumsaliti” kabla hayajatukia, ili wapate kuamini ya kuwa YEYE NDIYE Masihi. Unabii mara zingine tunaugundua wakati umeshatokea ili imani yetu ijengwe kwa Mungu. Yeye ampokeaye mtumishi wa Mungu ampokea Mungu Mwenyewe.

*Omba, omba kwa bidii na bila kukoma, lakini usisahau kumsifu Mungu (Kusifu).
------------------------

Maswali: BWANA Kuosha miguu ya wanafunzi Wake inatupa fundisho gani? Kwa nini ni muhimu kujihoji kabla ya kula meza ya BWANA? Kwa nini wanafunzi walipaswa kuoshana miguu wao kwa wao? Je unaweza kuosha miguu ya mtu? Je, Petro alikuwa na nia njema aliposema asioshwe miguu? Je, mtu aweza kukaa kanisani ila awe na hila kama Yuda Iskariote aliyekaa na Yesu? Mkate uliomegwa unatukumbushaje kuhusu Yesu?

**SIKU YA 276.**
**(Oktoba 2)**

# Pasaka ya mwisho.

**Yohana 13.**



Pasaka haikuangukia wakati wa kifo cha Yesu kwa bahati nasibu, La! Pasaka siku kuu iliyoanza wakati Waisraeli walipotoka utumwani Misri, ilihusu kutoka utumwani mwa dhambi. Yesu Mwana-Kondoo wa Mungu alikuwa anakwenda kufa kwa ajili yetu sote binadamu, ili kutuokoa. Huu ulikuwa mwaka wa 31BK. Basi jioni Yesu na wanafunzi Wake 12 waliketi chakulani, pamoja. Nao wakiwa hapo Yesu alirudia tena "Amini, nawaambia mmoja wenu atanisaliti. Meza ya BWANA imeitwa pasaka ya mwisho, chakula cha mwisho, karamu ya kuagana, au Komunio.

Nao wanafunzi walihuzunika wasiamini, wakaanza kumwuliza mmoja mmoja "Ni Mimi BWANA?" Yohana aliyekuwa mdogo wa wote, alipenda kukaa karibu na Yesu. Japo wengine walipendwa pia, huyu alijisikia yu karibu zaidi kidogo na Yesu. Yesu akijibu swali hilo akawaambia la! Kwa wale ambao hawatamsaliti, ila alipokuwa akimpa chakula Yuda alisema "ni yeye niliyemchovia mkate Wake katika kikombe ndiye atakayenisaliti, Mwana wa Adamu aenda Zake, kama alivyoandikiwa; lakini ole wake mtu yule ambaye atamsaliti Mwana wa Adamu! Ingekuwa heri

mtu yule kama asingezaliwa kuliko kujiletea uangamivu ya namna hii." Wanafunzi walishangaa, hivi ni kweli nani, anayeweza kufanya uovu kwa Mwalimu wao mwema, anayewapenda. Yuda Iskariote yule mwenye kumsaliti, japo alijua ndiye mwenyewe naye aliuliza "Ni mimi Rabi?"

Yesu akamjibu "wewe wasema au ndiyo ni wewe." Basi Yesu akamwambia Yuda "uyatendayo uyatende upesi", Ila wanafunzi hawakujua kwa nini ameambiwa vile. Wengine walidhani kwa vile ni mhazini wa kikundi chao, pengine aliambiwa anunue mahitaji ya sikukuu au awape masikini kitu. Nafikiria kwamba Yuda kama mhazini alikuwa ameshughulikia kununua mwana-kondoo, na mkate, bali moyo wake ulikuwa mbali. Alikaa karibu na Yesu, kuonyesha yupo Naye bega kwa bega, akaendelea na udanganyifu. Akipokea tonge lile Shetani alimwingia na akatoka mara hiyo akaenda nje. Pengine nia yake haikuwa kwamba Yesu auwawe, bali alitaka afanye haraka kujitangazia ufalme naye apate kuwekwa kwenye cheo cha juu. Akaona Yesu anachelewa, basi akaona afadhali amsaidie kuharakisha mambo wasije wakakosa vinono. Je leo tunapenda mali au vitu au mambo mengine ambayo yanatufanya tuwe tayari kumwuza Yesu?

Mitume wote walikuja kwenye Pasaka au meza ya BWANA na dhambi au wivu, ila waliungamiana isipokuwa Yuda hakutaka kuungama. Tunaambiwa tuungame na kujihoji hata leo, kabla ya kupokea huduma ya ibada hii, hatujaambiwa tuwahoji wengine, au kuwahukumu. Huduma hii yatukumbusha tena upendo wa Mungu, kwani alikuwa tayari kumwosha miguu mtu atakayemsaliti. Naye Yesu akasema "sasa ametukuzwa Mwana wa Adamu Naye Mungu ametukuzwa. Enyi watoto wadogo bado kitambo kidogo Nipo pamoja nanyi, nanyi mtanifuata, kama Nilivyowaambia Wayahudi, niendako hamwezi kuja.

Yohana ametumia sura tano hivi kuandika yale ambayo Yesu aliyasema usiku ule. Basi akasema Amri mpya nawapa "MPENDANE kama vile nilivyowapenda. Watu wote watatambua nyinyi ni wanafunzi Wangu au watoto Wangu kwa jinsi mnavyopendana." Yesu hakusema watu watatambua ninyi ni wanafunzi Wangu kwa vile mnavyotoa sadaka, au kwa namna ambayo hampigi watu, bali watatambua mu wanafunzi, kwa jinsi mnavyopendana. Upendo hufunika wingi wa dhambi. Mtu anayependa ataogopa kumfanyia Mungu au watu ubaya.

Simoni Petro akauliza "BWANA unaenda wapi." Naye akamjibu anapoenda hawezi kumfuata sasa ila baadaye." Petro akazidi kuuliza akisema "Kwa nini nisiweze kukufuata sasa? Niko tayari kutoa maisha yangu kwa ajili Yako." Petro alikuwa na nia ya kufanya aliyoahidi kwa vile alimpenda Yesu Kweli, ila alidhani angeweza kumtetea Yesu na hata kufa kwa ajili Yake kwa kutegemea nguvu zake mwenyewe. Hakujua kwamba hilo linawezekana kwa neema tu pale atakapomtegemea Mwenyezi Mungu kumpa nguvu za kusimama imara. Ndipo Yesu alipomwambia Petro kwamba atamkana mara tatu kabla jogoo wa mapambazuko ya usiku huo hajawika mara mbili. Yesu akasema "Simoni, Simoni tazama Shetani ametaka kuwapepeta kama ngano, ili kutoa kujaribu uaminifu wenu Kwangu, ila nimekuombea wewe ili imani yako isitindikiwe, nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako." Yesu anatuombea hata leo.

Akawaambia wajitayarishe maana mambo yatabadilika. Watahitaji mkoba, nguo na hata upanga kwa ajili ya kujitafutia riziki. Na walipokuwa wakila Yesu alitwaa mkate ule usiokuwa na chachu au hamira, akaubariki na kuumega na kuwapa wanafunzi wake akisema "twaeni mle huu ndiyo mwili Wangu"; akatwaa kikombe na baada ya kushukuru alisema "nyweni nyote katika hiki, kwa maana ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi." Kunywa damu na mwili Wake inamaanisha kukubali Maneno Yake, na kufanya vile alivyotuamuru.
Yesu akasema hatakunywa tena sasa uzao huo wa mzabibu hata siku ile atakapokunywa mpya pamoja nasi sote kwenye ufalme wa Baba Yake, na Baba yetu mbinguni. Tumetafiti na kuona mvinyo uliotumika ni juisi ya mizabibu na si pombe ya mzabibu. Mvinyo au 'oinos' iliwakilisha zote mbili yaani juisi ya mzabibu na pombe ya mzabibu. Kujua ni aina ipi ilikuwa inakusudiwa itategemea sentensi ilivyokaa. Yesu akisema 'mpya' amemaanisha isiyooza. Twajua matunda yaliyooza yaitwa mvinyo au 'wine', nafaka iliyooza yaitwa bia, na viazi vilivyooza vyaitwa 'rum'. Hizi ni aina za pombe. Damu ya Yesu haiwezi kuwakilishwa na kitu kilichochacha au kuoza!

Yesu aliposema kwamba ile divai mpya au juisi ya mizabibu inawakilisha damu Yake imwagikayo kwa wengi kwa ondoleo la dhambi, haikumaanisha kileo au matunda ya kuoza. Kileo kina chachu, sasa kama mkate wenyewe haukutakiwa uwe na chachu hata kinywaji kisingepasa kuwa na chachu. Damu ya Yesu si ya kufanya watu walewe, bali waokolewe, ni alama (symbols) Takatifu, ikisimamia kutokuwa na hila yoyote au upotofu.

Asilimia arobaini ya wote wanywao pombe, wanakuwa walevi sugu, wanaoshindwa kukabili maisha yao, wagomvi, watelekezao familia, wasioweza kufanya vibarua au wanaohatarisha maisha ya mtu kwa kuendesha vyombo vya usafiri bila umakini. Ufunuo yasema walevi hawataingia mbinguni. Je, Yesu angewapa watu kitu cha kuleta shida kubwa kwenye jumuiya na katika umilele kweli? Kama mbwa wako angeuma watu 40 kati ya 100 (au watu wawili kati ya watano) wanaokuja nyumbani kwenu ungemfuga kweli? Pombe ina madhara mno, hatuamini kwamba Yesu kama Mnazarayo na Masihi aliitumia hiyo alipoishi.

Yesu hakuleta pombe au matunda yaliyooza kwenye meza Takatifu, na kusema inawakilisha mwili Wake mkamilifu na damu Yake kamilifu, hiyo ni kinyume cha mafundisho tunayoyajua kwenye Maandiko. Hiyo ni dhana potofu kwamba Yesu alitengeneza pombe, kitu ambacho sicho.

*Shetani Hawezi Kumshinda Mtu Anayeomba - Adui hawezi kumshinda mwanafunzi mnyenyekevu wa Kristo, yule ambaye anatembea kwa maombi mbele za Bwana. Kristo anaingilia kati Mwenyewe kama mlinzi/kivuli, kimbilio, dhidi ya mashambulio ya yule mwovu. Ahadi imetolewa, "Wakati adui atakapokuja kama mafuriko, Roho wa Bwana atainua viwango dhidi yake." ... Hakuna nguvu katika misukumo yote ya kishetani ambazo zinaweza kulemaza roho inayotegemea, kwa ujasiri yakinifu na sahili, katika hekima inayotoka kwa MUNGU

-------------------------------

Maswali: Yesu alisemaje kuhusu mkate na divai? Kwa nini mtu asionje pombe? Kwa nini Yesu alitaka tuchukue mkate na divai nasi? Mtume gani alisisitiza hatamkana Yesu? Amri mpya Yesu aliyotoa ilikuwa na maana gani? Je, mtu atajuaje kama fulani ni mwanafunzi wa Yesu? Je, mtu anaweza kuwa mshiriki wa kanisa bila kuwa mkristo? Je, divai na mkate inawakilisha nini? Kwanini ni vyema twende kanisani, au kuhudhuria ushirika unafuata Biblia?

**SIKU YA 277**
**(Oktoba 3)**

# Msifadhaikeni mioyoni mwenu.

**Yohana 14**



Yesu hakuwaita wanafunzi kwenye meza ya BWANA au mlo wa mwisho, kula pasaka tu, bali alitaka akae na kuzungumza nao kwa mara ya mwisho wakiwa pamoja. Yuda alipopewa tonge hapa ndipo aliondoka kwenda kwa makuhani aje na maaskari kumsaliti Yesu. Yesu aliwaita mitume 'watoto wadogo", unafikiri Kwa nini alifanya vile? Mitume walijua Yesu ni zaidi ya nabii, au rafiki yao, na siku hii aliwadhihirishia kabisa. Maneno ya sura hii yamewafariji waumini wengi waliofiwa, waliopata shida au dhiki za magonjwa, umaskini na hata kuachwa ukiwa na jamaa au marafiki wa karibu.

Yesu akiwa chakulani aliwaambia wanafunzi Wake wasifadhaike mioyoni mwao, na Maneno haya ni yetu pia, tusifadhaike, bali tumwamini Mungu na tumwamini Yeye. Akasema "nyumbani mwa Baba mbinguni mna makao mengi, kama isingelikuwa hivyo Ningewaambia." Kuna nafasi tele mbinguni, si kama tunapoenda safari, watu wanaweza kusema tumebakia na nafasi tano tu za watu! Akasema anaenda kutuandalia mahali pa kukaa. Wakati Yesu anajenga makao kule mbinguni, nasi hapa duniani tuzijenge tabia zetu zikomae kiroho kwa maisha ya mbinguni yasiyo na dhambi. Tabia zetu ndiyo kitu pekee tutakachokwenda nacho mbinguni, na wale watu ambao tumewaalika, hivyo kwa kila tunalowaza, tunalofanya au tunalotenda ni matofali ya lile jengo.

Tutakapopaa kwenda mbinguni hakuna atakayebeba sanduku, kompyuta, gari, nyumba, ndege, au chakula kwani huko viko vya kuvutia zaidi! Vile ambavyo macho hayajawahi kuona, wala masikio kusikia wala kuingia ndani ya mawazo ya binadamu. Tunapohamia kwenda mji mwingine hatuwezi kwenda kwenye pipa la taka na kuchukua mabaki ya vitu vilivyobomoka au kuchakaa tukaenda navyo mahali papya!

Wanafunzi walipata furaha maana wengi wao walikuwa hawana pa kukaa au nyumba, wakilala huku na kule. Hatujui kama majengo mapya yanajengwa, au pengine wale malaika waliofukuzwa kule waliacha sehemu nyingi za kuishi! Hilo hatujui, ila tujipe moyo, nafasi ni tele tele, za kila mtu kuingia na kubaki. Akasema akienda kuandaa atakuja tena atukaribishe Kwake, ili Yeye alipo nasi tuwepo. Akasema "Niendako mwaijua njia nanyi mtakuja siku moja." Yesu alikuwa hajaacha kuwa Mungu, alikuwa Mungu bado hata kazi Zake na miujiza zilimshuhudia.

Naye Tomaso mwanafunzi, akawa muwazi asitake kuwa gizani akasema "BWANA wacha tukwambie Kweli hatujui uendako, wala hatujui jinsi ya kufika." Huyu alikuwa jasiri, maana hata leo wengi hawajui njia ya kwenda mbinguni ila hawaulizi, wanaogopa, wanasita au wana mashuguli mengi wakitegemea watauliza kesho. Yesu alimjibu Tomaso "Mimi Ndiye Njia, Kweli na Uzima, mtu haji kwa BABA ila kupitia Kwangu." Yeye Ndiye njia ya kufika kwa Baba na Ukweli wa jinsi Mungu alivyo na hakuna anayefika kwa Baba bila neema ya Yesu kumpitisha kwenye hiyo njia. Kama tukimjua Yeye basi tumemjua Baba. Basi Yesu akamwambia Filipo kutokea sasa, waweza kusema kwamba wamjua Baba na umemwona.

Filipo akarudia kuuliza "BWANA utuonyeshe Baba, yatutosha. Yesu akahuzinika maana alikaa nao miaka mitatu na nusu, mchana na usiku, akasema "Filipo Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue? Aliyeniona Mimi amemwona Baba; inakuwaje unaniuliza nikuonyeshe Baba. Husadiki kwamba Mimi ni ndani ya Baba na Baba Yu ndani Yangu?" Yote ninayozungumza na kufanya ni kwa vile Baba yu ndani Yangu, msadiki hayo kwa yale yote ambayo nimetenda.

Mitume waliposadiki haya walikuwa karibu na kila mmoja wao, na mbingu zikaonekana zi karibu sana. Tujifunze uvumilivu wa Yesu, na kustahimli; tusiwe watu ambao ni rahisi kukata tamaa, tukiwa na marafiki wasiotuamini au tukikutana na mambo magumu, tumwombe Mungu atuvushe. Twaweza kuwa na wazazi, walimu au watu wa karibu ambao wanafanya maisha yetu kuwa machungu, hebu tuone Mfano wa Yesu, Mzazi wetu.

Akasema Yeye anayemwamini, kwamba ni Masihi, Yeye Naye pia kazi azifanyazo atazifanya, tena katika eneo pana zaidi kwani wataenda dunia nzima. Yesu Anasema, "mtakaloomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana." Akasema sisi binadamu wote watoto kwa wazee "tukimpenda tutazishika Amri Zake" Naye atamwomba Baba atuletee msaidizi Ambaye ni Roho Mtakatifu. Japo Roho Mtakatifu haonekani kwa macho, tukimpokea atakuwa ndani yetu na atakuwa faraja kwetu, hivyo hatutakuwa yatima bila uongozi au faraja, mpaka Yesu atakapokuja kutuchukua. Yesu leo anaishi mioyoni mwetu kupitia Roho Mtakatifu.
Kwa sababu Yesu alifufuka na kuwa hai, nasi tutakuwa hai siku moja na tutaishi Naye milele. Roho Mtakatifu alitolewa kuwa mwalimu kutufundisha Maandiko yote, atatueleza yale ambayo ni dhambi, na yote ya haki. Atatuonyesha Mafundisho ya Kweli na ya uongo, ili tuchague ya Kweli na kuishi nayo. Karama au zawadi ya Roho Mtakatifu ni muhimu na ndiyo kitovu cha maisha ya mkristo. Mkristo mpya anazaliwa kwa Roho Mtakatifu na kuongozwa na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu Ndiye msaidizi wetu.

Yesu akasema anampenda Baba Yake na kila anachomwamuru hukifanya. Yesu alisema dalili ya kuonyesha sisi ni wafuasi Wake, ni kuwapenda wengine. Kama hatupendi kaka, dada, baba, mama au binadamu hatuna sehemu Naye. Je, wewe unapenda watu? Tukipenda watu, na kumpenda Mungu na kutii Amri Zake, atafanya mioyo yetu kuwa maskani Yake. Je, unataka kufanya moyo wako kuwa maskani Yake, na kutumiwa na Roho Mtakatifu?

Yesu akiwa na mwili wa binadamu, hakuweza kuwa pahali popote akiwa duniani, bali Roho Mtakatifu Yupo kwa kila mtu, kwa wakati wote. Hata kama tupo kifungoni au tumetengwa, Roho Mtakatifu yupo pale pamoja nasi. Mara nyingi tuna wazazi au mazingira magumu ya uovu, ila Mungu atatusaidia kujikwamua kutokana na hayo. Ili tabia Yake iwe ndani yetu. Yatupasa tusalimishe mioyo na nia zetu kwa Roho wa Mungu ili afanye kazi ndani yetu. Akili za mwanadamu ni finyu kuingiza mambo mengi, ila Roho Mtakatifu Yesu aliahidi atakuwa msaada kutusaidia kuelewa Neno Lake na kutukumbusha tuliyosoma.

Yesu aliwaambia mitume Wake siri ya ushindi itakuja wakimwomba kwa Jina Lake lenye nguvu na uwezo. Wakiomba kwa dhati, hata kama maombi yao yataonekana ni pungufu na hayana maneno ya kuridhisha, Roho Mtakatifu atayachukua na kuyapeleka mbinguni kwa Baba akiyapamba na manukato ya ukamilifu wa Yesu. Yesu ametuahidi hata leo, kwamba kwa Jina Lake, tukiomba atatujibu maombi yetu, kwa ajili ya haki ya Kristo. Yeye hutuombea kwa kuugua kwingi kusikotamkika, Tukimwuliza Yesu atusaidie tuwe na utii Kwake atatusaidia ili mioyo yetu na nia zetu vifanye Mapenzi Yake. Je, umempa Yesu moyo na nia yako leo? Ni Nani ana moyo wako? Mawazo yako yapo kwa nani? Je, unapenda kuzungumzia kuhusu nani au nini? Ni nani aliye na upendo wako wenye joto na nguvu zako bora zaidi? Ikiwa uko upande wa Bwana, mawazo yako yatakuwa Kwake Yeye! Muda wako, mali zako na burudani zako zitatumika kwa huduma Yake.

Je unafikiri ni jambo gani laonyesha Mungu anatuthamini? Je, si ni Kule kumtoa Mwana Wake wa pekee, aje atuokoe? Yeye anapenda sana tumwombe mambo makubwa, ili tufurahi na kumtukuza zaidi tupatapo majibu ya maombi yetu.
Je, ukienda kwa Rais wako na akakuruhusu uombe jambo, utaomba jambo dogo kama sindano au chungwa? Sidhani kama utafanya hivyo, maana hayo hata wazazi wako wangeweza kukupatia. Ukifanya hivyo kwa Raisi wa nchi yako ataona unamshusha hadhi yake. Mungu Naye Yupo hivyo; mwombe kwa imani mambo makubwa na tegemea makubwa toka Kwake. Tunapoomba kwa Jina Lake, pia tunapokea tabia Yake, na utii wa Kweli utokao moyoni. Hebu tumwombe ushindi huo.
Tukiamua katika maisha yetu kwamba hatupendi kumhuzunisha Mungu, basi tuje Kwake na mashaka au shida yoyote tuliyo nayo, Naye atatueleza cha kufanya, atatupa hekima ya kufanya mambo na hata nguvu na uwezo.

*Shetani Hawezi Kumshinda Mtu Anayeomba - Adui hawezi kumshinda mwanafunzi mnyenyekevu wa Kristo, yule ambaye anatembea kwa maombi mbele za Bwana. Kristo anaingilia kati Mwenyewe kama mlinzi/kivuli, kimbilio, dhidi ya mashambulio ya yule mwovu. Ahadi imetolewa, "Wakati adui atakapokuja kama mafuriko, Roho wa Bwana atainua viwango dhidi yake." ... Hakuna nguvu katika misukumo yote

ya kishetani ambazo zinaweza kulemaza roho inayotegemea, kwa ujasiri yakinifu na sahili, katika hekima inayotoka kwa MUNGU
-----------------------------

Maswali: Kwa niniYesu aliwaambia wanafunzi wasifadhaike? Je, twaweza kumwomba Mungu mambo gani? Kwa nini kushika Amri za Mungu ni muhimu? Je, ukimwambia mzazi wako leo kwamba huna haja ya kujali amri zake atakuambiaje? Je, Kwa nini Yesu si kama kiongozi yoyote wa dini, kama Budha au Dalai Lama? Kuna siku waumini husikia ukiwa, ila wao si yatima kwa sababu gani?

**SIKU YA 278**
**(Oktoba 4)**

# Yesu mzabibu wa Kweli.

**Yohana 15, 16.**



Yesu akatoa mfano akisema Yeye "Ndiye mzabibu wa Kweli, Baba Yangu Ndiye mkulima." Hii ilileta picha kichwani ya namna mti wenye matawi unavyofanya kazi. Mfano huo ulimaanisha, kila tawi lisilozaa huliondoa na kila tawi lizaalo hulisafisha au kulipunguza ili lichipue matawi mengi zaidi na kuzaa sana kama vile tupunguzavyo matawi ya miti ya matunda kama michungwa ili izae zaidi. Akasema kwamba Neno la Mungu ndilo pekee linafanya watoto wa Mungu kuwa safi, na mitume walikuwa wamesafishwa kwa Neno la Mungu.

Akasema "kaeni ndani Yangu Nami ndani yenu, kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu", kadhalika tusipokuwa ndani ya BWANA hatutazaa. Yeye akaaye ndani ya Yesu na Yesu ndani yake huzaa sana. Maana pasipo Yeye hatuwezi kufanya lolote. Na mtu asipokaa ndani Yake hukauka na kisha hutupwa nje motoni kama matawi ya kahawia yaliyonyauka yakateketea. Matawi yasiyozaa tunda la roho kama upole, upendo, furaha na uvumilivu, yatatupwa.
Tukikaa ndani Yake, tutakuwa na matunda mema. Majani hayana haja ya kushughulika sana ili yazae matunda, ni sehemu ya urithi Wake.Vivyo hivyo wanafunzi wa Yesu wanapojenga imani Kwake na kumtegemea ni dhahiri watajikuta wanazaa matunda kwa sababu ya rutuba inayotoka kwa Yesu. Sawa na mti unaotoa matunda kwa sababu ya rutuba inayotoka kwenye udongo mzuri.

Akasema tukikaa ndani Yake, Naye ndani yetu "ombeni mtakalo lote lolote nanyi

mtatendewa.” Kukaa ndani Yake ni pamoja na kushika na kutii Maagizo Yake. Utii wa kweli unatoka moyoni, na tukiomba kwa Jina Lake atatusaidia kumtii, na kujitoa kikamilifu. Atatupa hekima ya kufanya kile ambacho ni chema. Mungu anatukuzwa tukiwa ndani Yake na si kujiengua na kukaa wenyewe peke yetu. Twapaswa tukae ndani Yake ili tuwe wanafunzi Wake. Mungu anatupenda na hivyo tukae katika pendo Lake, na kuzishika Amri Zake. Mtu anayezivunja au kupinga Amri za Mungu ni mwongo wala hampendi Mungu.
Mungu ametupa Amri Zake kwa vile anatupenda. Amri Zake ni tumpende Yeye na na sisi tupendane. Yesu alitupenda mpaka akafa kwa ajili yetu. Tumekuwa marafiki za Mungu tukifuata Maagizo Yake na kumtii na “kila tumwombalo Baba kwa Jina la Yesu atatupa.” Ni rahisi kujichomeka kwa watu wengine, badala ya kuwa ndani ya Yesu. Hebu jiulize leo, u ndani ya Yesu au umejichomeka kwa watu wengine? Kwa maneno mengine unafuata mafundisho ya Maandiko na kumpendeza Mungu, au unafuata mafundisho ya binadamu wengine.

Yesu akawatahadharisha kuhusu mateso mtu anapomwamini. Watu wa ulimwengu waweza kutuchukia maana walimchukia hata BWANA Yesu. Mtumwa si mkubwa kuliko BWANA wake. Kama walimchukia Yeye, sisi je tutaepukanaje? Akatoa tahadhari kwa waumini wote kwamba watu wenye chuki na Mungu watakavyowatenda, hata katika masinagogi watawaua wale wanaompenda Mungu Kweli wakidhania wanatii Maagizo ya Mungu kumbe ni Shetani anawatuma. Sauli aliyegeuzwa kuwa Paulo alikuwa hivi, akififikiri kwa kuua Wakristo anamtendea kazi Mungu, kumbe alikuwa ametoka nje kabisa. Yesu akawaambia, asipoenda Zake, Yule mfariji Roho Mtakatifu hawezi kuja, huyo atawaongoza na kuwatia katika Kweli yote.

Yesu hakusema nao kwa mifano baada ya hapa; akawaambia alivyotoka mbinguni na kuja ulimwenguni, kisha wanafunzi wakasema “Tazama, sasa wasema wazi wazi, wala huneni kwa mithali tena……sasa twasadiki ulitoka kwa Mungu.” Yesu na BWANA wetu akifurahi akawauliza “Mnasadiki sasa?” Ndipo akasema saa imefika ambao kila mmoja wenu atatawanyika kwake, na kumwacha peke Yake, walakini “Baba Yupo pamoja Nami. Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani Yangu. Ulimwengu mnayo dhiki na shida nyingi, lakini jipeni moyo, Mimi nimeushinda ulimwengu.”

Tukumbuke Maneno ya Mwisho ya Yesu; Yeye ni njia yetu ya kwenda mbinguni, bila Mwokozi hatuwezi kuokolewa. Yeye ni Kweli, wasiompokea hawana Kweli, Yeye ni uzima, hakuna atakayekuwa na uzima wa milele bila Yeye, ni muhimu leo, tukisikia habari hii njema tumpokee. Tukifuata Mafundisho Yake na kufuata Amri mpya aliyotupa ya kupendana kama alivyotupenda, daima tutakuwa watu wenye furaha. Yesu akawapa Maneno ya mwisho mitume akisema bado kidogo hamnioni tena, bado kitambo kidogo nanyi mtaniona. Kwa sababu naenda Zangu kwa BABA. Yesu akawaambia watahuzunika ila huzuni yao itageuka kuwa furaha. Hata nasi leo tuombe kupokea Roho Mtakatifu, na tumwombe BABA wa mbinguni Neno lolote moja kwa moja, ili furaha yetu iwe timilifu. Yesu daima alipenda kujikita kwenye Somo hili la Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni Mungu nafsi ya tatu, na kazi Zake, chukua muda kuzipeleleza leo.

Hatuwezi kufanya lolote jema bila kuvuviwa Naye. Yeye sasa ni msaidizi wetu. Msaidizi kamwe si neno linaloashiria mapungufu ila lina utajiri mwingi na kina cha ajabu. Yesu alivuviwa na Roho Mtakatifu kila siku ili afanye kazi Yake, na twaona Roho wa Mungu kwa mfano wa hua akibatizwa. Hatuwezi kufanya lolote bila Roho Mtakatifu. Hebu nasi kama Yesu leo tukite mawazo yetu kwenye Roho Mtakatifu.

*Maombi Huleta Nguvu za kupinga Jaribu -Tusipoomba bila kukoma na kukesha kwa bidii, tuko katika hatari ya kuzembea zaidi, na kuchepuka kutoka katika njia sahihi. Kila wakati adui anatafuta kuziba njia iendayo kwenye Kiti cha Rehema, ili tusipate neema na nguvu ya kupinga majaribu kwa ombi la dhati na imani.

*Shetani anaogopa kwa kutetemeka tukiwa tunaomba - Kuna nguvu kubwa katika maombi. Adui yetu mkuu anatafuta kila mara kuiweka roho inayofadhaika mbali na MUNGU. Ombi kwenda Mbinguni la mtakatifu mnyenyekevu zaidi linaogopwa na linampa kutetemeka na hofu Shetani kuliko amri za mabaraza au maagizo ya wafalme.

-----------------------

Maswali: Yesu alisema Yeye ni nani? Kukaa ndani ya Yesu kuna maana gani? 'Jipe moyo, maana ameushinda ulimwengu' ina maana gani kwako leo? Twawezaje kuwa marafiki wa Mungu? Kwa nini Yesu alifurahi wanafunzi waliposema wanamsadiki? Orodhesha kazi 10 za Roho Mtakatifu.

**SIKU YA 279.**
**(Oktoba 5)**

# Sala ya Yesu kwetu wote.

**Yohana 17, Luka 22**



Usiku ule Yesu aliomba ombi zuri la ajabu kwa ajili yako na yangu. Mitume wote wengine walisahau kuliandika isipokuwa Yohana, ombi hili ulisome mwenyewe kwenye Yohana 17. Yesu alisema alitaka sisi wote tunaompenda na waumini tuwe kitu kimoja kama YEYE na BABA Yake walivyo na umoja. Umegundua kwamba ombi hili ni mimi na wewe tu, ndiyo tunaweza kulijibu au kulitimiza? YEYE hawezi! Hebu tumpe uchaguzi au nia zetu. Hata leo Waafrika husema ukitaka kwenda kwa haraka nenda peke yako, ukitaka kwenda mbali nenda na wengine!

Watu wengi hufikiri watu wa makabila, dini, umri, rangi, utamaduni mwingine, au watu wa hali au mahali fulani, ndiyo wana ubaguzi ila wao wanapenda umoja hili si kweli. Kila binadamu ana ubaguzi fulani! Ukikaa na kuchunguza utagundua ila jambo muhimu ni kuongoka na kuazimia kwamba Neno la Mungu ndiyo dira, na kinga ya ubaguzi. Hapo ndipo tutajaa upendo na kuwa na umoja ule wa kumpenda jirani kama nafsi, na anapopatwa na shida unaumia moyoni na kuwa na huruma japo hamna mahusiano ya damu naye.

Nimemwomba Mungu anisaidie ili nipende watu kama vile ninavyojipenda mwenyewe. Hii itafanya kazi ya Roho Mtakatifu ya kuwaambia wengine habari njema za ufalme kuwa rahisi, kwani tutapatwa na huzuni tukitambua kwamba watu wengine watapata adhabu kwenye ziwa la moto, na watatokomea milele zote tusiwaone tena, ikiwa hatutawaambia Ukweli. Kamwe, hata adui mbaya tusimtakie machungu ya kuogelea kwenye ziwa la moto.

Kristo hakutaja madhaifu yao, au ujinga wao, au wivu waliofanyiana. Aliwaambia kwamba huzuni yao itageuzwa kuwa furaha. Akasema furaha itajaza mioyo na mawazo yao, kiasi kwamba maisha yao hayatakuwa vile yalivyo tena. Japo imani yao iliterereka, na wakakimbia, Yesu alijua udhaifu wao, na wala hakuwakatia

tamaa. Aliwakusanya tena na kuwatuma mpaka miisho ya dunia wakafanya mambo makubwa kwa Jina Lake. Akawaambia wawe na furaha, maana Yeye ameshashinda na atagawana nao ushindi Wake. Hata leo imani yetu ikiwa ndogo, tusikate tamaa, Yesu hatuachi, anajua shida zetu hata tukiteleza, atatuinua. Tumkiri Yeye tena na kusonga mbele tukimwomba nguvu za kushinda. Kwani ameshatugawia ushindi Wake, tunapoomba tuwe na nia Yake iliyotajwa kwenye Wafilipi sura ya pili.

Akizungumza na Babaye, yale mazuri tu kuhusu marafiki Zake, alimwomba Baba Yake awatunze na kuwaangalia daima. Alisema, wote ulionipa wawe na uzima wa milele. "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma." Ni furaha ya namna gani tukitambua kwamba ombi hili halikuwa kwa mitume wale 11 tu, bali kila mtu anayempenda Yesu. Sote sisi alikuwa anatuombea, wewe na mimi, ili tulindwe na yule mwovu, ili mioyo yetu iwekwe sawa na kujazwa upendo, ili siku moja tuwe Naye milele zote mbinguni.

Yesu akainua macho yake mbinguni na kusema kwamba "saa imefika, nimekutukuza duniani, na nimeimaliza kazi, ile uliyonipa niifanye. Na sasa Baba mtukuze Mwanao, ili Mwana Wako Naye akutukuze Wewe." Akamwambia Babaye kwamba kazi aliyomtuma ameimaliza. Kazi ya kudhihirisha tabia ya Mungu kwa wanadamu, na Maneno aliyompa wanafunzi na wengi wameyapokea, na kujua hakika kwamba alitoka mbinguni Kwake BABA Mungu. Akaombea wanafunzi Wake na sisi sote mpaka mwisho wa dunia ili tulindwe na mwovu asije kutunyakua. Akaombea tuwe na umoja sisi tunaompenda wote duniani, kama Yeye alivyokuwa na umoja na Baba wa mbinguni. Akasihi "usiwatoe katika ulimwengu, bali uwalinde na yule mwovu." Kisha akasema maneno mazito na matamu kwetu sisi sote "Baba hao ulionipa (ambao ni mimi na wewe), nataka wawe pamoja Nami popote Nilipo, wapate na kuutuzama utukufu Wangu ulionipa." Yesu alitujulisha ni Emanueli, yaani Mungu pamoja nasi.

Alipofika bustani ya mizeituni aliwaambia wanafunzi ombeni msije mkaingia majaribuni, akijua wataingia katika shida karibuni wasijitegemee, waombe msaada kila mara toka kwa BWANA. Akajitenga nao kwa kiasi cha kutupa jiwe akapiga magoti akaomba "Ee Baba ikiwa ni Mapenzi Yako, uniondolee kikombe hiki; walakini si Mapenzi Yangu bali Yako yatendeke. Yesu alijua kitakachotokea usiku ule, utesi hata mpaka kutundikwa kwenye miti, akajisikia Yupo Mwenyewe, kubeba mzigo huu, Yeye asiyewahi kufanya dhambi, alihukumiwa na waovu.

Yesu aliomba hadi jasho la damu likamtoka. Kukosewa haki si jambo dogo. Je, umeshawahi kusingiziwa jambo, hata dogo tu, na ambalo hujafanya? Ulijisikiaje? Yesu alikuwa anaenda kulaumiwa na kutuhumiwa kwa mambo makubwa na mazito zaidi ambayo hakuyafanya. Dhambi kubwa kubwa, za kuua, dhambi zote zilizotendeka toka kwa Hawa mpaka mwisho kutoka Hawa bustani ya Edeni mpaka leo zilibebeshwa juu Yake. Haikuwa tu kifo ndicho kilimdidimiza au kumfanya moyo Wake upondeke, bali dhambi na mzigo, wa dunia.

Kama angekufa moyo na kukata tamaa saa ile, tungepotea milele. Alikuwa ana majaribu makuu, kwani angeweza kutokomea kwa muujiza kama vile alivyofanya

watu wa Nazareti walipotaka kumwua. Alikuwa anaenda kuchukua aibu yote inayohusiana na dhambi, Mungu alimwekea dhambi yetu yote, ndiyo maana Mwokozi alikuwa na huzuni kuu. Hapo ndipo Malaika toka mbinguni akamtokea akaja kumtia nguvu. Alipokuja upande wao alikuta wamelala maskini, Naye akahuzunika moyo. Alikuwa umechoka na alihitaji mfariji na wanafunzi wa kumsaidia kuomba, walikuwa wamelala usingizi. Akawaambia tena "Amkeni mwombe, msije mkaingia majaribuni." Hata leo twapaswa kuomba ili kuepuka majaribuni, hata kama tu watoto wadogo. Tusitoke kwenda shule au kulala bila kuomba, twahitaji kuomba asubuhi na jioni na hata mchana. Mtu mmoja amesema kutokuwa na maombi kwa saa moja, ni hasara! Yesu aliona utengano mkubwa na Babaye kwa ajili ya dhambi. Kuokolewa au hatima ya dunia, ilikuwa kwenye mizani, kwa kile kilichokuwa kinakwenda kutokea masaa machache.

Nao walipokwisha kuimba, wakatoka nje kwenda mlima wa mizeituni. Na walipofika ng'ambo ya kijito cha Kedroni penye bustani, akaingia Yeye na wanafunzi Wake. Naye Yuda aliyemsaliti alijua yuko huko maana alikuwa akienda na wanafunzi Wake mara nyingi. Aliienda na kikosi cha askari na watumishi wa wakuu wa makuhani na mafarisayo na taa, na mienge na silaha. Yesu alijua yatakayompata alipowaona aliuliza "Mnamtafuta nani?" Nao wakajibu Yesu mnazareti? Naye akawaambia "Ni Mimi hapa." Kisha wakashangaa walipomwona Yuda akisimama pamoja na wale askari. Yesu alipowaambia "ni Mimi" walirudi nyuma wakaanguka chini kwa ule utukufu wa Mwana wa Mungu. Kuanguka huku kulitokea mara mbili.

Yuda akamkaribia Yesu na kumbusu busu la unafiki. Alikuwa amewaambia wale wakuu ishara ndiyo hiyo "nitakayembusu Ndiye huyo mkamateni." Naye Yesu akamwambia "Yuda wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu." Yuda alimpenda Yesu, ila yaonekana kwamba alipenda mali na wadhifa zaidi ya YESU. Je kuna unachopenda kuliko unavyompenda Mungu? Mitume waliokuwa pamoja naye, walimwuliza Yesu kama wawapige hawa kwa mapanga, na Petro akampiga mtumishi wa kuhani aitwaye Malko na kumkata sikio la kuume. Yesu akasema "Acheni msifanye hivyo, je, kikombe alichonipa Baba Yangu Mimi nisikinywee?" Akachukua sikio na kulibandika tena, yule mtumishi akapona. Yesu akasema watu wanaotumia mapanga hufa kwa mapanga, akamwambia Petro arudishe silaha yake alani. Nafikiri Malko aliacha kuendelea na kazi hii ya uovu, baada ya sikio lake kuponywa. Wayahudi waliopenda ishara waliona ishara mbili usiku ule, ila hazikuwasaidia.

Yesu aliwaambia wale watu wawaache huru marafiki Zake yaani wanafunzi Wake, ili litimie Weno "Alionipa sikumpoteza hata mmoja." Yesu ametufundisha ufalme Wake si wa mapanga na silaha, bali nguvu kuu ya upendo. Alikuwa na uwezo wa kuita malaika maelfu waje kuzima uovu wa watu hawa ila hakufanya vile ili Maandiko yatimie. Hapa ndiyo tunaona Maandiko ni ya muhimu. Yesu alijitoa kikamilifu, yaani asilimia mia moja akimtii Mungu na kufuata Maandiko. Yesu alijua makuhani ambao walikuwa Masadukayo, ndiyo walitoa kibali cha kumkamata akawauliza makuhani wakuu, maakida wa hekalu na wazee waliokuja "Je mmekuja wenye panga na marungu kama kukamata mnyanganyi? Kila siku Nlipokuwa nanyi hekaluni hamkuninyoshea mikono, ila sasa ndiyo saa ya mamlaka ya giza."

Makuhani walikuwa na chuki na uovu na wakafikia kikomo kwa kwenda kinyume cha sheria za binadamu na Mungu ili wamtoe Yesu kwenye macho yao. Hawakupenda kusikia Kweli ili watubu. Walifikiri Yesu akifa watakuwa na raha katika maovu yao. Kifo cha Yesu kinatuletea raha na furaha, bali tusipojisalimisha Kwake, ni hatari mno. Yesu alikuwa na jaribu ambalo sisi binadamu hatuwezi kupitia, nalo ni kutumia uwezo Wake wa kiungu ili kushinda majaribu. Alikana nafsi Yake na kuitalawa hata walipomcheka na kumpiga, hakurudisha majibu machafu au mabaya.

*Kila nafsi ina upendeleo wa kumwambia Bwana mahitaji yake maalum na kuleta shukrani zake binafsi kwa baraka ambazo hupokea kila siku.
----------------------------


Maswali: Mtumishi Malko alipata shida gani?  Ombi Lake Yesu kuu kwa Baba Yake ilikuwa ni nini usiku ule? Je unafikiri Petro angeingia majaribuni endapo angekesha na kuomba usiku ule? Kwa nini umoja aliotuombea Yesu kabla ya kuuwawa ni muhimu kwetu? Je umoja huu twaweza kuwa nao tukiwa na mafundisho kinyume cha Maandiko Yake? Kwa nini Yesu aliomba wanafunzi Wake wawe na umoja? Kwa nini Yesu alikuwa na majaribu ya kushinda wanadamu wote? Je mtu anawezaje kuacha lugha chafu au kububujika matusi?

**SIKU YA 280.**
**(Oktoba 6)**

# Yesu anakamatwa.

**Luka 22**

Usiku ule wa manane Wakamkamata Yesu wakamchukua nyumbani mwa kuhani mkuu mstaafu Anasi maana alikuwa mkwewe Kayafa, ambaye ndiye aliyekuwa kuhani mkuu mwaka ule. Hawa wote walikuwa masadukayo. Yaani hawakuamini ufufuo, wala viumbe vya mbinguni kama vile Malaika. Kayafa ndiye alitabiri "Yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu." Kuhani huyu akajiona yeye ni shujaa sasa, kwamba ndiye anaenda kuliokoa taifa la Israeli kwa uwezo wake, na kumbe anapotea na kupoteza watu kwa kumwua Asiye na hatia kwa chuki. Cheo, mamlaka, utajiri na elimu vimetumika duniani kutawala wengine na kubadilisha mafikara yao. Makuhani walitaka kuharibu mafikara ya watu wa kawaida wasimpokee Yesu na kumpenda. Wengine walifikiri kwamba makuhani hawawezi kukosea, wakawafuata makuhani na viongozi wao wa kanisa jambo lililosababisha kupotea kwao.



Hata leo kuna makuhani wengi wanaomfuata Yesu, bali kazi hiyo ina majaribu makubwa, Ibilisi anapenda kukwaza wale wanaomtumikia Mungu, maana wale wanaomtumikia wapo upande wake tayari, hana haja ya kuwakazania. Ufalme wa Mungu ni kuwa mtumishi, hata malaika ni watumishi japo wameumbwa na wadhifa wa juu zaidi yetu.Cha kujifunza hapa ni ile hali ya kutaka kufanya kazi ya Mungu kwa kulipwa. Yaani fedha unaiweka mbele. Uwe tayari kufanya kazi ile kwa moyo wako, ukimtegemea Mungu, na kujitahidi kufanya yale ambayo hata usilipwe Mungu Ndiye anaona. Na walei yaani watu wanaomtumikia Mungu bila kulipwa, wawe makini kutoingia kwenye siasa za viongozi wa dini, maana hawapewi mshahara kwa siasa. Hawa watatoka mikono mitupu na zaidi ya yote watamchukiza Mungu, watakosa vyote.

Kuhukumiwa kwa Yesu hakukuwa halali kutokana na sheria za Kiyahudi. Baraza lao la Sanhedirini halikupasa kukutana na kumhukumu mtu usiku. Isitoshe ilikuwa

kinyume cha sheria mtu kufunguliwa mashtaka, kuonekana mwenye hatia na kisha kuhukumiwa afe kwa siku moja hiyo hiyo. Wayahudi walikuwa wamevunja sheria yao wenyewe, kwa kumhukumu Yesu ila jazba ya chuki iliwajaa. Waliona wivu kwa jinsi Yesu alivyopenda, alivyoponya, alivyopendwa, alivyofundisha mambo mazuri, na hivyo kufanya Mafundisho yao yakaonekana yamepauka, na ya uongo. Huenda kulikuwa na watoto wachache mahakamani usiku ule. Nahisi wale dogo (young) walioponywa na Yesu wangekuwepo pale, mambo yangekuwa tofauti. Huenda wangejaribu kumtetea! Ila watoto wote walikuwa vitandani, wamelala fo! fo! fo!.

Tunaposema Wayahudi hawakuwa na haki, ni upande wa uongozi zaidi. Walikuwa wamemchukia Yesu na wakamwogopa, kwa kuwa aliwafanya waonekane ni waovu wenye hila. Walitaka waharakishe na hukumu ipite haraka kabla watu wengi waliompenda Yesu hawajaamka na kuleta ghasia au kuona uovu wa makuhani wazi wazi. Walishaamua wamwue hata bila ya kesi kufanyika, ila walitaka tu waonekane wamepitia sheria kidogo ili waonyeshe walifanya mambo kihalali. Wayahudi wangemhukumu kwanza kisha Warumi. Wakijua sababu zao hazitoshi kumhukumu kifo, walianza kazi hii mapema ili watimize lengo lao. Walitaka wamhukumu kwamba anamkufuru Mungu na hilo ni kosa kwa sheria za Kiyahudi, kisha wakataka kuonyesha ni mhalifu anayeleta uasi ili ahukumiwe kifo kwa sheria za Kirumi.

Yohana alimfuata Yesu pia, naye alikuwa amejulikana na Kuhani mkuu akaruhusiwa kuingia behewani. Petro alimfuata kwa mbali, na walipokwisha washa makaa ya moto katikati ya kiwanja maana ilikuwa usiku wa baridi. Petro aliketi nao akiota moto, ndipo mjakazi wa kike alipomwona Petro ameketi mwangani akamkazia macho akisema “na huyu alikuwa pamoja na Yesu”, Petro alikana akisema “Eh mwanamke, mimi simjui Yesu.” Haikupita kitambo mwingine akamwona na kusema “wewe nawe u mmoja wa wafuasi wa Yesu.” Petro akasema “Eh mtu si mimi.” Ikapita saa moja na mtu mwingine akaja na kusema “Hakika na huyu alikuwa pamoja na Yesu, yeye pia ni Mgalilaya maana hata lafudhi yake au usemi wake unamtambulisha.”

Naye Petro alikuwa amekana kwa mara ya tatu “Eh Mtu sijui usemalo.” Papo hapo akiwa katika kusema, jogoo wa pili akawika. Na Petro alikumbuka Neno lile BWANA Yesu alilomwambia “Leo kabla hajawika jogoo mara mbili, utanikana mara tatu.” Akatoka nje na kulia machozi kwa uchungu. Masikini Petro, alimpenda Yesu, ila alitumainia nguvu Zake kusimama. Alisinzia wakati ambapo angepaswa kukesha aombe ili apate nguvu za kumshinda mwovu. Hata leo tunahitaji kusimama kwa nguvu za Mungu.

Yesu alijua yote, ndiyo maana akamwombea Petro ili imani yake isitindikiwe. Hata kama alimkana Yesu, Yesu hakutaka akate tamaa na kuikana imani yake. Wale waliomshika Yesu walimfanyia dhihaka, wakamsujudia Yesu na kumkejeli, wakamtemea mate na wakampiga makonde, mijeledi na makofi. Walimfunika macho na kumwuliza “tabiri ni nani amekupiga?” Jambo la huzuni, kwamba Mwumbaji aliyekuja kufa kwa ajili yetu, alifanyiwa dhihaka kubwa. Walimtolea maneno mengi ya dhihaka, na kumtukana. Wakiendelea kuzungumza kesi hiyo usiku, kinyume cha sheria za nchi hiyo; wakakutanika wazee, wakuu wa makuhani, na waandishi wakamleta katika baraza yao wakimwuliza habari za Mafundisho yake na wanafunzi

ake wakisema “tuambie kama Wewe ni Kristo.”

Akawaambia, hana haja ya kurudia maana hayo yote aliyasema wazi wazi siku zote na hata akisema hawatasadiki, kabisa. Aliwaambia, “tena Nikiwauliza hamtajibu, lakini tangia sasa Mwana wa Adamu atakuwa ameketi upande wa kuume wa Mungu Mwenyezi.” Akawaambia wawaulize wale waliosikia Mafundisho Yake, hapo ndiyo mtumishi wa makuhani alimpiga Yesu kofi, akitaka amfurahishe mkuu wake akasema “wamjibu kuhani mkuu hivi?” Masikini asijue kwamba hapa kuna Mkuu zaidi ya Malaika. Naye Yesu alisema “kama nimesema ubaya ushuhudie ule ubaya, bali kama nimesema vema, wanipiga nini?” Anasi akawaambia “mpelekeni kwa mkwe wangu.”

Wale watu walioleta baraza yaani makuhani, wazee, waandishi na mafarisayo waliuliza “Wewe Ndiwe mwana wa Mungu? Akasema “Ndiyo mmesema sawa.” Yesu ilibidi ajibu swali hili, kwani liliwapa wengine nafasi ya wote pale kujua ile Kweli na kufanya maamuzi kumfuata. Kamwe asingeweza kuliepuka, ila wao wakajitia kupata ghadhabu kwamba wana haja gani tena ya kuwa na ushuhuda maana “sisi wenyewe tumesikia Maneno ya kinywa Chake.” Walizungumza mengi, bali hayakuwa na ushahidi, si kwa sababu tu hakuna aliyeyaona, ila hayakuwahi kutokea. Yesu aliwajibu hawa kwa uvumilivu, na bila kuwa na hasira nao.

Yesu alifanyiwa mambo ya aibu na wale ambao alikuwa anajitoa kufa kwa ajili yao. Shetani na jeshi kubwa la malaika zake walikuwa pale kuwasukuma watu kutenda maovu na kuweka ghadhabu zote kwa Yesu. Shetani alikuwa anaenda kupata pigo kubwa na la mwisho. Malaika yoyote angeweza kumtoa pale, ila Baba wa mbinguni na Yesu waliamua watoe hii kafara ili mimi na wewe tusipotee bali tuwe na uzima wa milele. Ulikuwa wakati mgumu kwa Yesu kwani alijua kwa ndani kila kitu kinachoenda kutokea. Isitoshe ilikuwa kwa mara ya kwanza BABA Yake alinyamaza au mawasiliano yalionekana yametokomea. Kule kuonekana kuondoka kwa ukaribu au uso wa Mungu, ndiyo lilikuwa pigo zito kwa Yesu kupita yote.

Kwa vile Wayahudi walikuwa hawana mamlaka ya kumwua mtu, maana walikuwa chini ya utawala wa Rumi,Yesu alichukuliwa kutoka kwa Kayafa mpaka kwa Praitoria (ukumbi wa mahakama ya Kirumi) nayo ilikuwa alfajiri. Alikuwa amekaa zaidi ya masa 24 bila kulala. Wayahudi hawakuingia kwenye praitoria wakihofia kutiwa unajisi na hivyo kuwazuia wasile pasaka, wasijue kwamba dhambi wanayoifanya ni kubwa, na ilishawatia unajisi zamani. Walikuwa wanapanga mipango ya kuua, hiyo ilitosha kuwaletea unajisi.

Kila mtu alipewa nafasi ya kumkiri Yesu, na Mwenyezi Mungu siku ile. Iwe ni Kayafa, Anasi, Herodi, Pilato, mafarisayo, waandishi au raia wa kawaida; ila uovu wao ulikuwa umefikia kileleni, kwa kuwa walikuwa wameacha kumsikiliza Roho wa Mungu, na kuchagua kutawaliwa na roho ya mwovu.

*Hayatoi Habari Mpya kwa MUNGU- Maombi au Sala havieleweki kama inavyopaswa kueleweka. Kusali sio kumpasha MUNGU habari ambazo Yeye hazijui. Bwana anazifahamu fika siri za kila roho. Maombi yetu hayapaswi kuwa marefu

na yenye sauti ya juu (kubwa). MUNGU anasoma mawazo yaliyofichika ndani. Tunaweza kuomba kwa siri, na Yeye anayeona kwa sirini atasikia, na atatupatia thawabu hadharani.


---------------------------

Maswali: Mtu aliyempiga kofi Yesu angegundua Yeye ni nani angefanyeje? Twawezaje kumpiga makofi leo Yesu? Kwa nini makuhani walianza kesi usiku wa manane? Kwa nini Wayahudi hawakuwa na mamlaka ya kumhukumu mtu kifo? Anasi alikuwa nani? Kwa nini Petro alimkana Yesu ingawa alimpenda sana? Twajifunza nini kwa Yesu aliposhitakiwa bila kufanya kosa? Jadili ulilojifunza kuhusu viongozi hawa wakubwa wa kanisa, na husisha na maisha yako ya leo.

**SIKU YA 281.**
**(Oktoba 7)**

# Yesu kwa Pilato.

**Luka 22.**



Wakasimama mkutano wote wakampeleka kwa Pilato ambaye alikuwa mtawala wa Kirumi; pengine walimwamsha usingizini. Haikuwa halali watu hawa kumhukumu mtu usiku, ila walikuwa wana haraka kutenda uovu, wakisema kwamba siku kuu ya Pasaka inakuja nao yabidi waharakishe sana, ili watimize uovu wao haraka wa kumwua YESU. Twaweza kushangaa Kwa nini walifanya uovu huu, ila hata leo sisi tunafanya vile vile, na kumsulubisha Kristo upya kwa dhambi tunazotenda, tuombe Roho Mtakatifu, tugundue na kubadili njia kwa toba na matengenezo. Herode Myahudi alikuwa chini yake Pilato. Wayahudi wasingeweza kumhukumu wao wenyewe na Herode, kwa sheria ya nchi.

Pilato alishangaa kukuta Yesu ni mtu mpole, na mwungwana naye aliwauliza “mashitaka gani mnayoleta kwa Mtu Huyu?” Wakasema Ana mambo mengi tu, la sivyo wasingemleta kwako. Wakaanza kumshitaki wakisema uongo kuwa Amepotosha taifa lao, na kuwazuia wasimpe Kaisari kodi; akidai Yeye ni Kristo na Mfalme. Wengine walisema aliwaambia Atabomoa hekalu na kulijenga baada ya siku tatu. Alimradi ushuhuda wao haukupatana. Pilato akamwuliza “Wewe ni Mfalme wa Wayahudi?” Yesu akimpa Pilato nafasi ya wokovu, akajibu “ndiyo kama unavyosema, ila unauliza kwa wokovu wako mwenyewe au watu wengine walikuambia habari Zangu?” Pilato akasema “ama, mimi si Myahudi, watu wa taifa Lako na makuhani ndiyo walikuleta.”

Pilato akamhoji Yesu akamwambia ufalme Wangu siyo wa ulimwengu huu, la sivyo watumishi Wangu wangepigana nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi.” Yesu aliendelea kumshuhudia Pilato, kwamba amezaliwa kwa ajili ya haya, akampa kisa cha wokovu na Kweli ile Yesu anaiyoshuhudia. Pilato akauliza swali “Kweli ni nini?” Swali hili mimi na wewe tunapaswa kujiuliza leo, “Kweli ni nini?” Kweli ni

Neno la Mungu tu! Ndiyo Kweli yote, na Kweli tupu (absolute Truth). Basi Pilato akawaambia wakuu wa makuhani, na makutano "Sioni Neno lililo ovu kwa mtu Huyu." Aliwaambia wamtwae wamhukumu kwa sheria yao, ila wakasema "sisi hatuna ruhusa ya kuua mtu." Wayahudi walikazania wakisema mtu Huyu huleta shida nyingi akifundisha katika Uyahudi yote, tokea Galilaya.

Pilato aliposikia aliuliza kama anatoka Galilaya, Naye akamwambia ndiyo. Akaona yupo chini ya mamlaka ya Herode, akampeleka Yesu kwa Herode maana naye alikuwa amekuja kutembea Yerusalemu. Herode huyu ndiye aliyemwua Yohana mbatizaji. Herode alipomwona Yesu alifurahi sana, kwa sababu alikuwa amesikia habari Zake, na alitaka kumwona siku nyingi. Alimwambia Yesu amfanyie ishara na miujiza aliyosikia iwe kama burudani. Yesu hakuja duniani kufanya michezo ya kuigiza au mazingaombwe. Akamwuliza Yesu maneno mengi, ila Yesu hakumjibu lolote. Wakuu wa makuhani na waandishi wakasimama wakamshtaki kwa nguvu sana.

Herode kwa chuki, na kwa vile alikuwa na mamlaka, akamfanya Yesu duni machoni pa watu, bila ya kujali wadhifa Wake. Akamdhihaki kwa kumvika mavazi makuu-kuu ya zambarau ya kifalme, kisha akamrudisha kwa Pilato kwani naye kama Pilato hakuona hatia. Hili ni fundisho kwetu kutomdhihaki au kumzomea mtu. Tokea siku ile ile, Herode na Pilato walipatana kwa urafiki kwa maana hapo kwanza walikuwa na uadui. Kupatana kwao hakukuwa "adui wa adui yangu ni rafiki yangu." Bali Herodi aliafikiana na Pilato kwamba Yesu hana kosa. Hata leo wengine wamemwuza Yesu ili wawe marafiki na watu fulani waliokosana nao siku za nyuma.

Pilato akiwa kwenye kiti cha hukumu, mtumishi akaja na ujumbe toka kwa mkewe kuhusu ndoto aliyoota usiku ule "Usiwe na neno na Yesu maana ni mtu wa haki, kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili Yake." Ila hili halikusaidia. Pilato aliendelea kuwapendeza watu ili asiharibu kibarua chake. Pilato aliwaambia wale wakuu wa makuhani Kayafa na Anasi, kwamba wamemleta Mtu huyu eti anapotosha watu. Naye akajibu akisema, "nami nimeamua mambo yake mbele yenu, sikuona Kwake kosa lolote katika mambo hayo mliyomshitaki, ni uongo tu." Hata Herode hakuona uovu Wake wowote. "Hakuna Neno ovu lolote ambalo Yesu ametenda linalostahili kufa." Akasema atamrudi kwa kumpiga viboko kisha atamfungua, maana iliwalazimu kuwafungulia mfungwa mmoja wakati wa sikukuu naye aliamua kumfungua Yesu na kumwacha huru. Hakika ni kisa cha ajabu, kama mtu hakupatikana na kosa lolote, kwanini basi umpige viboko? Ila Wayahudi walipiga kelele wakisema "Mfunge Yesu na umfungulie Baraba." Jina la Baraba lilikuwa na maana 'Mwana wa baba.' Jamaa zake walikuwa wamesikia anaenda kuuwawa. Alipewa habari msalaba wake unachongwa. Huyu alikuwa ametupwa gerezani kwa uasi uliotokea mjini na kwa mauaji aliyofanya. Baraba alisikia jina lake likitajwa akiwa jela. Akahofu kifo kimefika, mara akaona mlango umefunguka. Baraba katika ujana wake lazima atakuwa mtu aliyewapa shida wazazi wake. Alijitafutia vijana wa hovyo na kushirikiana nao.

Baraba akapelekwa kwa Pilato, akamwona Naye Yesu pale, pengine alimjua au kusikia habari Zake. Pilato akasema nao mara ya pili, kwamba anataka kumfungua

Yesu naye akawauliza, “Nimtendeje Yesu Aitwaye Kristo?” Lakini Wayahudi walipiga kelele “Msulubishe, msulubishe.” Baraba akafurahi. Hatujui kilichomtokea alipotimua mbio kama mtu huru siku ile. Tunatumaini kwamba naye aligundua amepona kwaajili ya Yesu kukichukua kifo chake kama sisi leo. Yaani kwa kupigwa Kwake, na kifo Chake Yesu, sisi wenye dhambi tumepona. Basi najua tunaendelea kujiuliza tena na tena! Je, alimpokea Yesu, Yule aliyechukua kifo chake cha wakati ule na cha pili? Je alirudia maisha ya zamani? Hatujui! Baraba anasimamia kila mtoto, na mtu mzima leo. “sote ni wana wa Baba” kama Baraba. Hapa wakisema Wayahudi wanamaanisha wale watu waliokuwa na nia mbaya.

Wale watu waliοponywa na Yesu na kusaidiwa, na hata marafiki Zake wengi hawakushiriki kwenye uovu huu. Pilato akauliza mara ya tatu, “Kwa sababu gani? Yesu ametenda uovu gani? sikuona Kwake hata neno lipasalao kufa, basi nikishampa adhabu ya kumrudi nitamfungua.” Nao Wayahudi walijibu kwa nguvu sana wakitaka asulubiwe, sauti zao zikashinda. Pilato akahukumu, haja yao ya uovu ndiyo ifanyike, nao wakijua wanataka kuharakisha ile hukumu, wakamfungua yule aliyetupwa gerezani kwa ajili ya uasi na uuaji. Yule Baraba waliyemtaka, akamtoa Yesu wamfanyie watakavyo akinawa mikono akisema “Mimi sina hatia ya damu ya Mtu huyu wa haki.” Maji ya dunia yote yasingemsaidia kutoa uovu wake wa kumwua Masihi, isipokuwa kuungama dhambi. Wayahudi wote pale wakajibu “damu Yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu.” Kamwe hakuna aliyeona dhambi au makosa kwa Yesu, hata maadui Zake, hii ni tofauti na viongozi au waanzilishi wa dini nyingine zozote, wenyewe na waliowaona walikiri kwamba walifanya dhambi au kukiuka yale waliyofundisha. Hili lipo wazi, kwani ni Mungu tu asiyetenda dhambi, wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

Hata leo tutazame mikono yetu, na tunapofanya uovu au dhambi yoyote ni mikono yetu inamsulubisha Yesu tena. Hebu tuombe msamaha maana dhambi zote Yesu husamehe. Pilato japo alipewa bahati ya kujua Ukweli au ile Kweli, alitaka kuridhisha watu, japo alijua Yesu hana hatia alimpiga viboko, naye ndiyo kiongozi, hakuna ambaye angemwambia kwa nini hukumpiga Yesu viboko. Wayahudi walikuwa wamemchagua Baraba aliyewakilisha ufalme wa Shetani badala ya Yesu. Leo sisi ni kama Baraba, tumeachwa huru, na Yesu akafa kwa ajili yetu.

Mke wa Pilato, alituma ujumbe kwa mumewe, kuhusu ndoto ya kutisha. Waweza kubahatisha kwamba ndoto hii iliyotoka kwa Mungu ilisemaje? Pengine ilielezea kuhusu Yesu ni nani, na maisha Yake mpaka atakaporudi mara ya pili. Basi wakati Pilato yupo mahakamani, alipewa onyo na mkewe “Usiwe na neno na Yule mwenye haki; kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili Yake.” Ila bado Pilato alisonga mbele asirudi nyuma. Na bado akijua Yesu hana hatia kabisa alimpiga viboko. Tunarudia kwa nini umtendee jeuri au hiana mtu Asiye na hatia kama si kuridhisha watu na kujaribu kutunza wadhifa wake? Wengi walimjua Yesu siku zile kwa zile kazi Zake, na yawezekana hata mama huyu akipewa ndoto, alikuwa ameshawahi kusikia kuhusu Yesu na huduma aliyofanya au hata jinsi atakavyokuja mawinguni siku ya mwisho; hili halikumsaidia Pilato. Ufunuo 1:7 yasema atakaporudi mawinguni, kila jicho litamwona, hata wale waliomtendea uovu. Mungu aturehemu ili tusimtendee Mungu uovu, na tukitenda tuombe msamaha.

Mungu alitumia njia zote, amwokoe Pilato pia, ila alikuwa mtu dhaifu na mwoga apendaye kufurahisha watu ili asipoteze wadhifa wake. Yesu angekufa hata bila Pilato ila sasa Pilato alikuwa na hatia kwa kuwa hakutumia nafasi yake kama hakimu kumuokoa asiye na hatia. Je, twapata fundisho gani toka katika maisha ya Pilato? Wanahistoria walisema Pilato alipoteza kazi ile baada ya kifo cha Yesu japo alijaribu kupendeza watu. Waandishi Tasitasi na Yosefasi (Josephus) ni miongoni mwa wanahistoria walioandika mengi zaidi kutuhakikishia yalitokea baada ya kifo cha Yesu. Ukipata nafasi waweza kujisomea mwenyewe.

*Yesu hatuiti tumfuate, na kisha atutelekeze. Ikiwa tusalimisha maisha yetu kwa ajili ya huduma Yake, hatuwezi kamwe kuwekwa katika nafasi ambayo MUNGU hajaandaa majaliwa Yake. Katika hali yetu yoyote, tuna Mwongozo wa kuongoza njia yetu; shida zetu zozote, tunaye Mshauri wa kweli;huzuni yetu yote, kufiwa, au upweke, tunaye Rafiki anayetuhurumia. Ikiwa pasipo kujua au ujinga wetu tunafanya makosa, Kristo hatuachi

*Maombi rahisi yaliyosukuwa na Roho Mtakatifu yatapanda kupitia malango wazi, mlango ulio wazi ambao Kristo ametangaza: Nimefungua [47], na hakuna mtu anayeweza kufunga. Maombi haya, yaliyochanganywa na uvumba wa ukamilifu wa Kristo, yatapanda kama manukato kwa Baba, na majibu yatakuja.
---------------------

Maswali: Pilato aliona makosa gani kwa Yesu? Mke wa Pilato alimpa tahadhari gani? Kwa nini watu walimchagua Baraba badala ya Yesu? Je, Hata leo watu wanamchaguaje Baraba badala ya Yesu? Kwa nini Herode na Pilato walipatana siku ile? Kwa nini Pilato alimpiga Yesu viboko hata bila makosa? Yesu anatupa mfano gani wa uvumilivu watu wakitutendea maovu? Je Unapenda kuridhisha watu leo, au kumridhisha Yesu!

**SIKU Ya 282.**
**(Oktoba 8)**

# Taji ya miiba.

**Yohana 19.**



Pilato akijua fika, Yesu hana makosa, akitaka awafurahishe Wayahudi na atunze hadhi na kazi yake basi alimtwaa Yesu na kumpiga mijeledi. Nao askari walisokota taji ya miiba wakamtia kichwani, wakawa wakimwendea na kumkejeli "Salamu! Mfalme wa Wayahudi!" Wakampiga makofi, wakamvika vazi la zambarau la kifalme kumkejeli. Pilato aliogopa na dhamira ikamshtaki, kwani alijua Wayahudi wamemtoa Yesu kwa chuki tu. Hata hivi leo mtu akifanya dhambi, ambayo si uhalifu, hatuwezi kumlazimisha awe muumini kwa kumpa adhabu au kumwua. Kuwa muumini ni uchaguzi wa mtu, tunapaswa kumwambia mtu akiwa amefanya dhambi au kosa, tukitumaini atatubu na kuacha njia yake ya uovu ila hatumwui.

Kamwe katika hali tunayoishi leo, hakuna kiongozi wa dini aliyepewa mamlaka ya kumwua mtu mwenye dhambi ambazo si makosa ya jinai au uhalifu mfano mzushi. Mfano akitokea leo mtu na kuzusha kwamba yeye ni Mungu, ila asimtendee mtu yoyote baya, kanisa au serikali haipaswi kumwua. Na hata hivyo binadamu gani asiye na dhambi, kwa maneno mengine wataua watu wangapi? Basi itabidi watu wote

wauwawe! Basi Pilato akamwuliza Yesu "Wewe umetoka wapi?" ila Yesu hakujibu, na Pilato kwa kukasirika alisema "huzungumzi nami? Hujui ya kuwa mimi nina mamlaka ya kukufungua nami nina mamlaka ya kukusulubisha?" Yesu akamjibu, mamlaka yote yatoka juu, na hata yeye asingepata mamlaka kama asingepewa na Mwenyezi Mungu.

Tangu hapo Pilato alitaka amfungue Yesu lakini akashindwa, maana Wayahudi walimwambia "ukimfungua wewe si rafiki wa Kaisaria, naye akiwa mtu mwenye kutaka kutunza cheo chake, akaamua asimfungue. Yesu alikaa penye sakafu ya mawe, na Pilato akasema "Tazama Mfalme wenu. Watu walimjibu "Mwondoshe hapa msulubishe." Shetani alitamani Yesu afanye dhambi katika kipindi cha maisha Yake, bali alishindwa. Hapa alitaka Yesu ajibu ovyo, au kufanya jambo la kumwangusha, ili ashindwe. Shetani alitumia mbinu zote alizoweza, hata mateso makali ya viboko vya chuma na vipande vya mifupa, ila Yesu alistahimili yote ili sisi tuokoke.

Pilato alipata wakati mzuri wa kuzungumza na Yesu mpaka akajua ile Kweli yote ya Neno la Mungu inayotosha kuokoa maana Mungu alimtumia mkewe ndoto. Yesu ni Njia, Kweli na Uzima. Sidhani kama Pilato angekufa kwa njaa au mahitaji ya lazima, kwani alikuwa raia wa Rumi. Shida ingekuwa hadhi yake kupungua, na wakasema yeye hatakuwa rafiki wa Kaisari, kwani watamchongea! Wengi wanamwuza Yesu leo kwa ajili ya marafiki, michezo, woga, fasheni, urembo, maoni, cheo, maslahi, sifa, shule, umashuhuri, hadhi au bidhaa za bei ya chini au chenji chenji. Kila binadamu anapitia vishawishi kama hivyo. Ni swala la kujihoji kila mmoja wetu. Je, wewe unamwuza Yesu kwa michezo na wenzako? Kutazama mikanda ya televisheni au picha chafu? Kusikia nyimbo za ovyo zisizojenga kama rap, ngono chafu au kuzungumza maneno yasiyofaa? Tuombe Mungu atusaidie sana kwani kwenye mabasi mengi picha chafu huwekwa ili watoto na watu wazima waone, picha ambazo zinadhalilisha wanawake wa Kiafrika, na kuwatukuza wanawake wa nchi zingine, picha ambazo hazina kanuni safi bali uasherati, na uzinzi. Picha hizi zinakiuka utamaduni wetu ila ni za watu mashuhuri wanaoishi maisha ya giza na hivyo vijana wanaendelea kuharibikiwa. Yesu alikufa kwaajili yetu ili tuponyoke kutoka kwenye uovu huu, nawe jitahidi kuwaambia watu wenye mabasi waweke aina nyingine ya mikanda na si ile yenye ukatili, na uchafu unaoharibu moyo. Siku moja tukiwa kwenye basi, mama mwenye watoto wa miaka mitano hivi alipomwambia kondakta, alikaripiwa kwa kuambiwa "waambie watoto wako wainame chini". Sijui watoto wangeinama chini kwa muda gani, kwani safari yetu ilikuwa refu, yaani kutoka Nairobi kuelekea Mwanza! Hakika tungependa siku ya hukumu ambayo i karibu inapokuja tusimame kama washindi. Hivyo twapasa kulinda njia za moyo, tuonayo, tusikiayo, tugusayo, tunusayo, yawe yachujwe kutokana na Wafilipi 4:7-8, Kichujuo bora kuliko vyote kwa kila mwenye mwili ni hiki:
"7 Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.

8 Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya Kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.
9 Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu,

yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi."

Yuda aliyemsaliti, alipoona Yesu ameteswa na amekwisha kuhukumiwa, hakuamini. Yeye alifikiri Yesu atatumia miujiza, awe huru. Alienda kwa makuhani kurudisha vile vipande 30 vya fedha. Akisema "Nalikosa nilipoisaliti damu isiyo na hatia." Wale makuhani walimwona sasa hana thamani kama kabla ya kuwafanyia kazi yao haramu, wakasema "Haya hayatuhusu sisi, beba mzigo wako mwenyewe ukaushughulikie." Hii ilikuwa ushuhuda wa hila za makuhani na rushwa waliyotoa ili uovu ufanyike. Yuda alitupa chini vile vipande 30 vya fedha, akaenda kujinyonga. Angeomba msamaha angesamehewa, ila alikuwa amemkufuru Roho wa Mungu kwa kutosikiliza sauti ya Mungu kwa miaka mingi. Petro siku ile ile alikuwa amemkana Yesu, ila aliomba msamaha na akawa shujaa wa Bwana.

Wakuu wa makuhani walitwaa vile vipande vya fedha na wakaona si halali kuviweka kwenye sadaka kwa kuwa ni pesa za damu zinazoendelea kuwashitaki. Wakazitumia zile fedha kununua konde la mfinyazi ili kuzikia wageni. Konde hilo likaitwa konde la damu, ili litimie Neno la nabii Yeremia. Yuda alikufa siku moja na Yesu, wote walikufa kwenye miti, Yesu msalabani; Yuda alijitundika kwenye mti. Yuda alijiua, na Yesu aliuwawa. Yuda alikufa kama msaliti, Yesu alikufa kama shujaa na Mwokozi. Yuda hakumsaidia mtu kwa kifo Chake, ila Yesu alituokoa wote siku ile. Wote tuseme, Haleluya, neno langu pendwa la Kiebrania!

Wengi siku ile walikuwa wamemsaliti Yesu kama Yuda ila waliungama. Kutojua si sababu ya kutosha kukuondolea dhambi au kufanya dhamira isikushitaki. Twapasa tujielimishe kuhusu mambo yahusuyo wokovu wetu. Mfano wa Yuda Iskariote umewekwa kwetu leo, kama onyo pale tunapomsaliti Yesu kwa matendo, au maneno yetu. Tuombeane sana kwani sote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Hakuna hata mmoja mkamilifu, sote tumeoza! Tamaa ya pesa na maisha haya imekuwa shimo ambalo wengi wameangukia. Yuda alipenda fedha na Mamlaka. Alifikiri kwamba anajua kuliko wengine, na japo Yesu alimpa nafasi ya kujisahihisha miaka hiyo mitatu hakuitumia vizuri. Watu wengi siku ile walijua Yesu ana tabia ya pekee, kwani alimvumilia huyu msaliti bila kumuumbua siku zote alizoishi pamoja naye.

Yesu alisulubishwa saa tatu asubuhi. Suluba ilikuwa adhabu ya Warumi kwa maharamia na wauaji. Yote haya aliyafanya kwa ajili ya dhambi zangu na zako, ili sisi tusio na uzima wa milele, tuweze kuishi Naye milele. Huu ni upendo wa ajabu. Akahesabiwa pamoja na waasi. Warumi walikuwa na utesi mkubwa, yule aliyetundikwa alibeba msalaba anaoenda kutundikiwa. Yesu alijichukulia msalaba Wake, mpaka mahali paitwapo fuvu la kichwa au Golgotha. Akiwa njiani alikosa nguvu, kwa kuchoka, kutolala, kupigwa, kuishiwa damu, na zaidi ya yote dhambi zetu. Wakamchukua Mwafrika aliyekuja Yerusalemu, aitwaye Simoni Mkirene, wa Libya, amsaidie. Huyu alikuwa anapita na watoto wake wawili, Iskanda na Rufo, akiwa ametoka shambani.

Pengine walimwona Yesu akiwa hana nguvu kwa mapigo na kupungukiwa na damu, maana alikuwa hajalala kwa zaidi ya masaa 24. Pengine Simoni alikuwa ameonyesha

huruma akimwona Yesu anapata mateso makali haya. Twaamini Simoni wakati akibeba msalaba huu, alipata nafasi ya kumjua Yesu naye. Nasi leo tunaulizwa kubeba msalaba, mdogo au mkubwa kwa ajili ya Yesu, Je uko tayari kufanya hivi kila siku? Wengi wakashangaa mtu anauawa bila kosa. Maelfu wakamfuata ili waone, maana kwa kawaida wengi hupenda kutazama au kushabikia, wakisikia jambo.

Wanawake waliomfuata wale waliosaidiwa Naye, na kumhudumia, walijipiga vifua, wakilia na kumwomboleza. Yesu aliwageukia akishukuru kwa huruma zao akasema "Enyi binti za Yerusalemu, msinililie Mimi, bali jililieni nafsi zenu na watoto wenu." Siku hizo za mwisho waovu watasema "milima tuangukie, na vilima tufunikeni." Wanawake hawa walikuwa wanamhurumia Yesu kwa huruma za binadamu, ila alijua kwamba wakimwamini kama Mwana-Kondoo achukuaye dhambi za dunia, ndiyo itakuwa msaada mzuri zaidi kwao. Nimefurahia Maneno haya ya Yesu kwani ametupa ruhusa sisi wakina mama na wazazi kwa jumla kuwalilia watoto wetu ili wasipotee, bali wawe na uzima wa milele nao siku moja!

Kuonea watu huruma katika shida zao ni muhimu, ila haitampeleka mtu mbinguni. Huruma pekee haitoshi, ila hiyo ni njia tu ya kufikiri kikubwa zaidi ya hicho. Kikubwa ni kumkubali Mwana wa Mungu kama Mkombozi, na Mwokozi wa maisha yangu, maana hakuna Jina ambalo tuwezalo kuokolewa isipokuwa hilo. Kuna wengi wanapapasa na hawana jinsi ya kujua ile Kweli sana kama wale walio na Maandiko. Na hao Mungu anawasaidia kwa machache wayajuayo na kuyatenda. Wengine kwa sehemu mbali mbali duniani wameonyesha huruma kwa wenye njaa, magonjwa, umaskini na mateso. Hawa wakiwasaidia watu wenye shida, wanakuwa wamemsaidia Yesu Mwenyewe.

Wakaweka ule mti chini, na kumpigilia misumari miguuni na mikononi, na kuusimamisha tena ule mti juu. Unaweza kupiga picha kichwani mwako, kupigilia misumari kwenye mkono, mpaka iende chini kwenye mti wa msalaba, na kutundikwa hivyo kwa siku nzima. Na nguvu ya uvutano itadai mwili uwe unashuka chini, ila misumari inajaribu kushikilia mwili. Basi wakamsulubisha huko, na wanyang'anyi wawili, mmoja kushoto, na mwingine kulia. Yesu hakusema maneno ya hasira bali "Baba uwasamehe kwa kuwa hawajui walitendalo." Ombi hili la Yesu ni kwa kila binadamu, kuanzia Adamu mpaka yule wa mwisho atakayeishi duniani. Yesu alikuwa na majeraha sita jumla, kila mkono na mguu ulipigiliwa misumari, ubavu ulipigwa mkuki, na paji la uso lilichomwa na miiba. Majeraha mengine ni yale ya kupigwa viboko vya vipande vya nyuma na mifupa yenye ncha kali. Wote tuna hatia ya kumsulubisha Yesu kwa matendo yetu, ila tunapewa msamaha. Na tusipokubali msahama huo basi tutapotea.

Maelfu ya watu na pengine mamilioni mwisho wa siku kuu ya pasaka, walikuwa wamesikia injili siku ile kutokana na ushuhuda wa Yesu, viongozi wote wa nchi kuanzia, makuhani Pilato, hadi Herode walisikia yote siku ile, ilibakia kukata shauri wamfuate. Haya yote yameandikwa kwenye historia na mwandishi Tasitasi wa siku zile. Basi Yesu alipoambiwa anywe siki wakati huu ili kupoteza maumivu alikataa kwani siki ni kama kileo. Alitaka mawazo Yake yawe shwari wakati huu wa tukio zito kupita yote duniani la kutukomboa sisi, ili Shetani asiharibu mawazo au mambo.

Watu walikaa wengi wakitazama makuhani wakuu, wakimfanyia dhihaka wakisema “ameokoa wengine, sasa na ajiokoe Mwenyewe kama Ndiye Kristo wa Mungu, mteule Wake.” Hata wengine wakang’aka Ah! shuka utoke kwenye msalaba. Hata mhalifu mmoja aliyesulibishwa pamoja Naye alimfanyia mzaha akisema “Jiokoe nafsi yako na sisi.” Mwenzake alimjibu “wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu hiyo hiyo?” maana aliona wazi wazi kwamba wao ni wahalifu wanapata haki yao, na Roho akamfungulia kujua Yesu ni Mwana wa Mungu.

Mwizi wa pili alitoa maneno ya muhimu ya mwisho akisema “Ee Yesu nikumbuke utakapoingia katika ufalme Wako.” Yesu alimwambia Amini, nakuambia hivi leo, utakuwa pamoja Nami kwenye uzima wa milele.” Mwizi huyu anawakilisha wengi waliofungwa magerezani, na wale walioacha maisha ya zamani mabaya na kumpokea Yesu hata kama ni saa ya mwisho ya maisha yao. Yesu alipata faraja kwamba hata katika kufa Kwake, watu wengine walikuwa wanaokolewa. Yesu bado alikuwa Mungu na nguvu za kusamehe dhambi pale msalabani, na Mamlaka yote, ila aliendelea na kifo kile ili wewe na mimi tupate uzima wa milele.

Chukua muda kujishauri na kufanya uamuzi, unaposoma kifo Chake cha ajabu leo. Mwamini, maana ndiyo njia Mungu aliyoichagua kwako, kupata uzima wa milele leo. Usifikiri kila mtu hupata nafasi siku ya mwisho anayokufa ili atubu kama mwizi msalabani. Bahati ya mwenzako usilalie mlango wazi. Wengine hawapati nafasi ya kuungama kabla ya kufa, wamekuwa wakiahirisha kujikabidhi kwa Yesu mpaka wanapoaga dunia. Mtu asikudanganye kwamba wazee tu ndiyo wanakufa, watu wa kila umri hufa, wazee, watoto na hata vijana. Naye Yesu anaweza kuja mtu akiwa na umri wa miaka mitano (5) au mia (100).

Pilato akaandika anwani kwenye ule msalaba “YESU MNAZARETI MFALME WA WAYAHUDI.” Basi wengi walisoma hayo Maneno kwani yaliandikwa kwa lugha tatu, Kiyahudi, Kirumi, na Kiyunani. Wakuu wa makuhani walimwambia Pilato asiandike maneno vile bali aandike “Yesu alisema, Mimi ni Mfalme wa Wayahudi.” Pilato kwa hasira na huku dhamira ikimshitaki, na akiwa hoi kwa kuchoka kwa hisia zake kutibuliwa, akasema, alichoandika ameandika, wasimsumbue zaidi, maana siku hii naye kwake ilikuwa ya kumfadhaisha kiasi cha kutosha. Pilato alikuwa na bahati ya kuwa na Ukweli mbele yake bali hakutambua. Na Wayahudi walikuwa na Masihi mbele yao bali hawakumtambua. Waandishi wanahistoria wanasema kwamba haikupita muda Pilato alipoteza kazi na mwishowe alijiua kutokana na maandishi ya historia.

Maandishi haya yakawa mahubiri maana siku ile watu walitoka nchi nyingi duniani kusherekea pasaka; nao walisoma maandishi haya na kuyalinganisha na Maandiko ya unabii kuhusu Masihi. Kuanzia kuchomwa ubavuni, nguo kugawanya, kupewa siku na kadhalika. Unabii wa Masihi umejirudia zaidi ya mara 127 kwenye Agano la Kale. Maelfu tunaona walibatizwa mara tu baada ya Yesu kupaa mbinguni, hii ilikuwa kazi ya Roho Mtakatifu katika kuwasadikisha watu kuhusu dhambi, haki na hukumu.

*Maombi ya Unyenyekevu, usahili na Imani kama ya Mtoto Yatajibiwa - "Ikiwa mtu yeyote ana kiu, na aje Kwangu anywe." Lakini atakayekunywa maji nitakayompa Mimi, hataona kiu milele. Maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji ya uzima na kumpatia uzima wa milele." Yohana 7:37; Yohana

------------------------------

Maswali: Yuda alipoona Yesu anaenda kuuwawa alifanyeje? Pilato aliandika maneno gani msalabani? Je Yuda alisikitika kwa kumsaliti Yesu au kwa kuwa mipango yake iliharibika? Unabii gani wa Masihi ulitimia siku ile ya kusulubishwa kwa Yesu? Kweli ni nini? Kwa nini ni jambo baya kumzomea mtu au kumkebehi kama yule mwizi wa msalabani alivyofanya?

**SIKU YA 283**
**(Oktoba 9)**

# Yesu anakata roho.

**Yohana 19, Mathayo 27**



Askari waliomsulubisha Yesu wakaachana na mambo ya kushughulikia wanaosulubishwa, wakaanza kutwaa mavazi ya Yesu na kuyagawa mafungu manne, kwa kila askari fungu lake na kanzu nayo. Kanzu ile ilikuwa haikushonwa, wala kuwa na upindo, wakaambiana wasiipasue bali waipigie kura, ili andiko litimie, "waligawanya nguo Zangu, na vazi Langu wakalipigia kura." Msalabani walisimama mamaye, umbu la mamaye Mariamu wa Kleopa, Mariamu Mgadalena na wanawake wengine, na Yohana. Kisha Yesu angali ametundikwa msalabani alisema kwa mama Yake "Mama Mtazame mwanao Yohana" na kwa Yohana alisema "Yohana mtazame mama Yako."

Yesu alikuwa Mwana aliyempenda mama Yake. Akijua ni mzee, alimtafutia mtu wa kumtunza hata wakati ule akiwa na uchungu mwingi. Yesu hakuwa na pesa za kumwachia mama Yake, bali Yohana aliyekuwa mwanafunzi Wake mpendwa. Yohana kuishi na Mama wa Yesu, kulikuwa baraka ya kumkumbuka BWANA wake Yesu. Mama huyu yaonekana alishakuwa mjane. Fundisho tunalipata leo, ni

kutowatelekeza wazazi wetu, kwa kuwatunza au kuwaheshimu. Japo Yesu alikuwa na ndugu wa mama mmoja kama Yuda na Yakobo, yawezekana hakutaka kuwaachia jukumu hilo kwani walikuwa hawajaongoka bado na kumpenda Mungu kama Yohana. Yasemekana Yohana alikuwa na undugu na Yesu pia; kwani mamaye, alikuwa jamaa wa Mariamu (kutokana na kulinganisha vitabu vitatu vya injili).

Mama Yake Yesu alipata majaribu na mitihani. Akakukumbuka toka alipotokewa na Malaika, mpaka Yesu alipozaliwa, alipitia uchungu wa mama. Hata Kuhani mzee Simoni alilisema hilo Kwake, akakumbuka. Akifikiri jinsi mtoto Wake alivyokuwa mwema na alivyokuwa tayari kuwasaidia watu akaona hakustahili. Unadhani ni kwa nini mambo haya yanatokea kama hivi? Mara zingine inabidi utengane na baba au mama yako, ila Mungu anajua. Uchungu Wake Yesu haukuwa wa misumari tu, bali wa dhambi za dunia yote, huo ndiyo ulimfanya afe mapema. Hatia za kuanzia Adamu mpaka mwisho wa dunia ziliwekwa kwa Yesu. Alitengwa na uso wa Baba Yake, na hii ilirarua moyo Wake kwa namna ambayo mwanadamu hawezi kuelewa au kueleza.

Uchungu huu ndiyo ukawa mzito zaidi ya ule wa mwili. Mungu BABA alikuwepo ila kwa ajili ya dhambi, kulionekana kuna utengo mkubwa. Hata leo dhambi zinatuficha tusione uso wa Mungu. Kuna siku dhambi itaondolewa na kukoma, ndipo tutamwona Mungu uso kwa uso. Hasira za Mungu sasa zilikuwa kwa Mwana Wake kama vile Isaya 53 inavyosema. Hata jua nalo likafifia kwa kuyaona mateso haya ya Muumba Wake. Yesu alipewa siki iliyochanganywa na nyongo kwanza, alipokuwa na kiu msalabani, alipoionja hii alikataa pengine kwa vile ina kileo, akitaka mawazo Yake yawe kamili mpaka mwisho.

Saa sita giza lilipotokea Yesu alipaza sauti Yake Akisema “Eloi, Eloi lama sabakthani”, maana yake “Mungu Wangu, Mungu Wangu mbona umeniacha.” Baadhi ya watu waliosikia walisema anamwita Eliya… Maneno saba yalirekodiwa, ambayo Yesu aliyasema akiwa msalabani. Yesu alisema msalabani “nasikia kiu.” Watu walimtukana matusi mbali mbali, na kumtemea mate, hata wale wezi pale msalabani. Majeshi ya Shetani yalikusanyika pale ili kuwatumia watu wafanye uovu, kwani walitaka Yesu atende dhambi kwa kujibizana nao na kufeli, ila ashukuriwe Mungu aliyejitwalia ushindi. Basi kupitia Yeye hata sisi tutashinda ila tuombe kuwa na tunda la roho hasa katika kutawala na kukana nafsi.

Jaribu alilopata Yesu hakuna binadamu ameshawahi kulipata au kupitia, kwani alikuwa na uwezo wote, nguvu zote. Kama angelitaka angaliweza kushuka msalabani na kuwashugulikia wale waovu wote kwa kuwapiga bakora. Bali hakutumia Uungu Wake kulazimisha watu kumtii!. Daima alifanya miujiza ya kuwasaidia wengine na si ya kujisaidia Mwenyewe. Hii tunaona hata alipokuwa na njaa ya siku 40 hakutengeneza chakula ili ajiridhishe nafsi Yake. Je Yesu angeshuka msalabani siku ile, sisi wenye dhambi si tungeangamia milele bila tumaini lolote?

Watu wote wanaomwamini Mungu wanapitia mateso mbali mbali. Tunaona kwenye Agano la Kale na Agano Jipya. Hata baada ya wakati wa mitume watu wengi wamepata mateso kwa ajili ya kumtetea Mungu na Neno Lake. Wengine

wametupwa kwenye matundu ya simba, wengine wamechomwa moto, wamepigwa viboko, wameharibikiwa majahazi, na wengine wameuwawa na majambia. Watu hawa kama vile Waldenses wa Italia, John Huss wa Chekoslovakia, Jerome, Knox na wengine wengi walipitia hali ngumu. Soma hitoria yao katika kitabu kiitwacho Pambano kuu na 500 martys. Hata leo nchi nyingi zinatesa waumini wanaomwamini Mungu. Twapasa kuwaombea, waishio kwenye eneo ambalo wengine huliita ukanda wa 'dirisha la 10 kwa 40.' Hizi ni nchi zilizomo kwenye latitude na longitude za kijiografia. Nchi hizi ni kama vile Korea ya kaskazini, Somalia na nchi zinginezo.

Giza lilipoingia saa sita mchana kwenye nchi lilidumu kwa masaa matatu. Watu wengine walipoliona hili pale msalabani siku ile ile waliamua kufuata njia ya uzima. Wengine waliingia na woga, wakifikiri wanapata malipo ya uovu wao siku ile. Basi Pazia la hekalu la urefu wa futi 60 na unene wa inchi sita hivi, lilipasuka toka juu kwenda chini lenyewe. Ikiwa binadamu angelitatua, angeanzia chini kwenda juu, bali ilikuwa ni kazi ya Mungu. Kupasuka kukatoa utengo kati ya mahali Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu ikionyesha kama isemavyo katika kitabu cha Waebrania kwamba sasa pale si Patakatifu tena, na kwamba watu wote kwa imani wako huru kumwendea Mungu moja kwa moja, kwa ajili ya ile kafara ya Yesu. Ile kafara Yake imefungua lile pazia kati ya mwanadamu na Mungu. Waebrania 7 mpaka 10. Hapa ni Waebrania 10.
"8 Basi, ondoleo la hayo likiwapo, hapana toleo tena kwa ajili ya dhambi.
19 Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia Patakatifu kwa damu ya Yesu,
20 njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani, mwili wake;
21 na kuwa na Kuhani Mkuu juu ya nyumba ya Mungu;
22 na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi.
23 Na mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana Yeye aliyeahidi ni mwaminifu;
24 tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri;
25 wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia."

Patakatifu pa Patakatifu tunapoonyeshwa kwenye kitabu cha Waebrania, sasa pako mbinguni. Kondoo waliokuwa wanataka kutolewa kafara siku ile wakakimbia kwa mtikisiko. Kukawa na tetemeko kubwa, makaburi yalifunguka na miili ya watakatifu waliolala wakafufuka wakauingia mji mtakatifu, na kutokea wengi. Mimi nina udadisi kwamba walikuwa nani, je! Wewe? Pengine Ibrahimu, au Yusufu, au Daudi, au Nuhu? Yesu akalia Neno la mwisho "Mikononi Mwako naiweka Poho Yangu." Kisha Akasema "imekwisha." Alipokwisha kusema hayo alikata Roho. Neno imekwisha au Tetelestai Kiyahudi lilikuwa Neno la ushindi mkubwa mbinguni, duniani na kwenye sayari zote. Huduma ya kutoa wanyama duniani ilikuwa imekwisha, sasa, Kristo Mwana-Kondoo wa Mungu alikuwa amekufa mara moja kwa ajili ya vizazi vyote kwa ajili ya dhambi zetu. Malaika waliokuwa na mashaka na hofu, nao wakajua hakika MUNGU ni UPENDO!

Yesu alikuwa na majaribu alipoishi ya kumfanya asiende msalabani, na Alipoenda msalabani alikuwa na majaribu ya kutoka kwenye ule mti, ila alikuwa ameshinda,

na aliposhinda, nasi tumeshinda. Turuke- ruke kwa furaha na kushangilia ushindi huo. Hata sidhani kwamba hivi leo wengi wetu katika siku hizi ngumu za uchumi na maisha ya mijini ya kileo, kama tungeweza kutoa zile kafara kama siku zile za zamani. Historia ilikuwa imebadilika, Yesu alikuwa amebomoa ukuta wa mahusiano yetu na BABA. Wanafunzi walikuwa na hofu na misongo siku hiyo, baadaye walipokaa na kurudia haya ndipo walipoyaelewa. Huzuni na uchungu mkubwa wa Yesu utupe mafundisho. Wakati mambo mabaya na machungu yanapotutokea watoto Wake, tusifikiri Mungu ametuacha, ila tukite imani yetu kwa Mungu, bila kujali hisia za hofu na uchungu tulio nao.

Yule akida au mwanajeshi alipoona yaliyotokea msalabani, alimtukuza Mungu akisema, "hakika Mtu Huyu alikuwa mwenye haki." Na wengine pia walikiri "hakika alikuwa mwana wa Mungu." Makutano wote waliokusanyika kutazama mambo haya walienda zao makwao wakijipiga piga vifua vyao. Wengi walikiri "hakika huyu ni Mwana wa Mungu." Yesu alikuwa amekufa kwa dhambi kwa moyo uliopondeka. Dhambi za dunia nzima, dhambi zako na zangu Yeye alizibeba. Shetani na Jeshi lake lote lilikuwa msalabani, kuanzia saa tatu mpaka saa tisa Yesu alipokufa; wakitaka nafasi ya mwisho kufanya mpango wa wokovu ushindwe, ila Yesu akashinda, Haleluya! Tuombeane kwenye Safari ili tuweze kufika!

Wote waliofahamiana na Yesu, na wanawake kutoka Galilaya wakasimama kwa mbali wakitazama mambo hayo. Wengine walianguka kwa hofu, kwa ajili ya giza, tetemeko au hata dhamira kuwashitaki. Giza lile na tetemeko kwa binadamu aliye na hekima ya mbingu, ilikuwa muda mzuri wa kutafakari mwenendo wa mtu. Hata pengine, watu walianza kuogopa Yesu aliyekufa, kuliko Yule aliyekuwa akitembea hai, maana nguvu za asili zilifanya maajabu siku ile. Wengine baada ya giza kutoka wakirudi makwao walifanya maamuzi ya uzima wa milele. Japo hakukuwa na magazeti habari hizi zilienea kote kwenye utawala wa Kirumi na ulimwengu uliojulikana.

Ni kwa ajili yangu na yako, kwamba Mwana wa Mungu aliamua kuchukua hatia ya dhambi, na kufa, ili ashinde mauti ya pili milele kwa mara moja na mara zote (once and for all). Ni kwa ajili yako na yangu, Alifungua malango ya mbinguni, kwa kutoa maisha Yake, kwa ajili ya upendo Wake kwako na kwangu. Tumshukuru Mungu daima kwa upendo huu wa ajabu, na kutafakari kifo Chake mara nyingi. Japo tuna masikitiko ya kifo Chake, ameleta matumaini kwetu na uzima wa milele. Yesu kwa kifo Chake alionyesha jambo jingine muhimu mno, nalo ni upendo mkuu wa Mungu kwa wanadamu. Mungu alifanya madai ya Shetani kuwa Yeye ni dikteta yaonekane ya uwongo. Shetani alikosa mashtaka dhidi ya Mungu.

Hata wale Malaika waliokuwa wanamtumikia Mungu baada ya Shetani kuasi, maswali yao yote yalijibiwa, na wakapata picha kamili ya upendo wa Mungu ambayo hawakuwa nayo hapo kabla. Sasa tabia ya Mungu imejulikana wazi. Kwa mashitaka yote Shetani aliyotoa, mbingu na dunia zimeona ni ya uongo, naye amejulikana tabia yake kama baba wa uongo na uovu wote. Mungu anatumikiwa tu na wale watu wanaochagua kumtumikia. Upendo waweza tu kuwa upendo kama tunaweza kuwa na uchaguzi. Mungu ametupa uchaguzi leo, kumtumikia Yeye au

Shetani. Kuna falme mbili tu, hakuna anayependa uovu, tunajikuta tu tumeingia. Hakuna anayetaka kuishi karibu na mtu mwovu, na ndiyo maana siku moja Mungu atatoa hukumu, ili uovu ufutwe milele zote. Yesu sasa ni kuhani, na mtetezi wetu ili siku ya hukumu tushinde. Hakuna kesi iliyowahi kumshinda, labda tumkatae asiwe wakili wetu wa kututetea. Muhtasari wa siku ile msalabani ulikuwa hivi: Yesu alipewa siki na kuikataa, Yesu akasulubishwa, Yesu akasema Baba wasamehe, askari wakanadi nguo Zake, Yesu akadhihakiwa na maadui na wezi walio msalabani, mwizi mmoja akamwamini na kuahidiwa atakuwa na uzima wa milele, Yesu amkabidhi mamaye kwa Yohana, giza kuu lilitanda nchi yote, Yesu akasema "Mungu wangu Mungu wangu mbona umeniacha, Yesu akasema ana kiu, Yesu Akasema imekwisha, Yesu Akasema "mikononi Mwako Baba Naiweka Roho Yangu", na mwisho Yesu akakata Roho.

Hebu fikiria basi, kwamba Mungu Mwenye hekima na uwezo wote hakuwa na njia yoyote ya kutuokoa isipokuwa kuja duniani na kupata mateso na fadhaa, Naye akaja na kuteswa na kufa. Hakika pambano hili kati ya wema na uovu ni kali sana. Na Kwamba Yesu anatupenda mno, kuliko tunavyofikiria. Yaani anatupenda Mno kuliko Anavyojipenda na tunavyojipenda Mwenyewe! Nafikiri hitimisho hili walikuja nalo kwanza malaika wa mbinguni! Hapo mwanzo wengine walijitenga na kumfuata Shetani, ila wale waliobakia hawakuwa na uhakika kuwa Mungu hakika alivipenda viumbe Vyake kiasi kile. Ila walipoona Yesu anateswa na kudhalilisha na Mungu hafanyi kitu, pengine walimwambia fanya kitu Bwana wetu asife au asipate fadhaa kiasi hiki, ila walipoona Yesu anafedheheshwa, anaumizwa na kisha kuuwawa, walipata mshtuko na mshangao papo hapo. Pengine hata walisema mioyoni mwao "Huyu Mungu jamani! Sisi tuko hoi, kwamba kwamba anawapenda hawa viumbe na pia sisi kiasi hiki? Kwamba anawapenda hawa binadamu kupita anavyojipenda Mwenyewe?" Hakika ni kitendawili kitakachosimuliwa milele zote na utamu na urojororojo wake usiishe milele zote! Yaani baada ya machafuko kuletwa na shetani, sayari zote na himaya yote ya Mungu ilikuwa hatarini mno, ila katika Hekima Yake Mungu, machafuko haya yameweza kutatuliwa, mara moja na milele zote. Hakuna ambaye anaweza kukataa au kupinga kwamba Mungu anatupenda kuliko anavyojipenda Mwenyewe!

*Ikiwa, pamoja na ahadi hizi mbele yetu, tunachagua kubaki wakavu na kuwa na kiu kwa kukosa maji ya uzima, ni kosa letu wenyewe. Ikiwa tungekuja kwa Kristo tukiwa na unyenyekevu wa mtoto anavyoenda kwa wazazi wake wa kidunia, na kuomba vitu ambavyo ameahidi, tukiamini kwamba tunavipokea, hakika tutakuwa navyo.

----------------------------

Maswali: Kwa nini Yesu alikufa? Yesu alimkabidhi mama Yake kwa nani? Maneno saba Yesu aliyosema msalabani ni yapi? Unabii wa Isaya 53 ulitimiaje siku ile msalabani? Je ni Mungu alimwua YESU? Kwa nini watu hawakuwa na haja ya kutoa kafara tena? Yesu aliposema imekwisha ni nini kilichokuwa kimekwisha?

**SIKU YA 284.**
**(Oktoba 10)**

# Mazishi ya Yesu.

**Luka 23-24, Marko 15, Mathayo 27.**



Imani ya wanafunzi wa Yesu ilikuwa imetikiswa, ila bado walimpenda sana Mwalimu na BWANA wao, ingawa ingekuwa vigumu kwao kupewa mwili wa Yesu ili wauzike. Basi hawakutoka pale msalabani ila wakangoja kuona kitakachotokea. Msaada ukaja kutoka mahali wasikofikiria. Kutoka kwa Yusufu na Nikodemu, Yusufu akatoa kaburi lake kwenye mwamba na Nikodemu akatoa ratili 100 za manukato. Kila mtu ana sehemu katika mpango mkuu wa kazi ya Mungu, hata wewe una sehemu. Yusufu na Nikodemu, walikuwa wanafunzi wa Yesu kwa siri. Walikuwa wamejitahidi kumlinda Yesu mara zingine wakati makuhani wakitaka kumwua. Waliogopa kujionyesha wazi wazi, ila upendo wao kwake, ila kifo cha Yesu kiliwabadilisha kuliko alipokuwa hai, nao wakapata ujasiri na kisha wakatoka mvunguni mwa kitanda. Hakuna mfuasi wa siri, siku moja itabidi atoke mvunguni! Tukimkiri Masihi mbele ya watu, Naye atatukiri mbele ya Babaye na watu pia.

"Akatokea mtu mmoja aitwaye Yusufu, mtu wa baraza la Sanhedrini, mtu mwema na mwenye haki, ambaye hakulikubali shauri na tendo la Wayahudi. Huyu alitoka mji wa Arimathaya, tena aliutazamia ufalme wa Mungu. Huyu alienda kwa Pilato, na akafanya ujasiri, na kwa siri kwa sababu ya kuwahofia Wayahudi akaomba apewe mwili wa Yesu. Hata leo twapasa kuchukua tahadhari tunapofanya kazi ya Mungu. Na jambo jingine la kukumbuka ni kuwa japo watu wanaonekana wana uovu, Mungu ana watu Wake wateule waliojikinga na mawaa au uovu kama Yusufu na Nikodemu watakaokuwa tayari kuifanya kazi ya Mungu katika mazingira maalumu. Pilato alishangaa Yesu alikufa mapema, maana kifo cha kusulubishwa kwa kawaidam watu huchukua siku chache kufa. Askari walienda na kuvunja miguu ya mhalifu aliyesulubiwa pamoja na Yesu, ila walipokuja kwa Yesu walimkuta ameshakufa.

Wayahudi huzika mtu akifa siku hiyo hiyo. Siku zile ndugu na marafiki waliishi karibu na kulikuwa na njia chache za kutunza miili. Kuvunja miguu ilimfanya afe mapema maana ilipunguza kujiinua katika jitihada za kutafuta pumzi. Wayahudi kwa desturi yao hawakuiacha miili imetundikwa vile siku ya Sabato au Pasaka. Wengine walifikiri miguu ilivunjwa ili 'wahalifu wasikimbie." Pilato Aliagiza Yesu achomwe mkuki wa mbavuni, na ikatoka damu na maji, ikimaanisha, hakika amekufa. Likatimia andiko la Zaburi "hakuna mfupa Wake utakaovunjwa" na "watamtazama Yeye waliyemchoma" mbavuni. Yohana alishuhudia hili na kuandika.

Pilato Alipopata hakika kwamba amekufa, alimpa mwili Wake Yusufu. Tunapata faraja kwamba Yesu alikuwa na marafiki wazuri kama Yusufu. Akasaidiana na Nikodemu aliyeleta manukato Kwake. Wakapanda ngazi na wakatoa misumari na kuushusha mwili. Kisha wakaufunga sanda ya kitani na kuuweka katika kaburi jipya lililochongwa mwambani. Heshima kubwa kwa Mwokozi ilitolewa, maana siku zile wale walioitwa wahalifu walizikwa kaburi moja, watu wengi. Watu walikuwa wamemchukia Yesu na kumpiga misumari, bali wengine walimpenda na kuiondoa ile misumari.

Kaburi hili limetembelewa na mamilioni ya watu toka kila nchi. Pengine Nikodemu akakukumbuka mazungumzo ya usiku ule "kama vile Musa alivyomwinua nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu ameinuliwa ili tusipotee bali tuwe na uzima wa milele." Hili likawa ushuhuda tosha kwake kukaza nia na kuwa mwanafunzi wa wazi! Wale waliohitaji kuponywa maskini, wakasikitika walipoona yote haya. Walikuwa katika hali tofauti sasa. Japo makuhani na watu wengine wenye hila walitaka watu wafunge midomo yao, kila mtu alizungumza kifo cha Yesu tena na tena kuliko hata akiwa hai. Wakapata hofu, kwani walimjua kuwa hajawahi kusema uongo, na kama alivyodai kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu wakadhani pengine angekuja na kulipiza kisasi. Tusiwe na hofu ya hilo, kwani wanaomwamini na kuungama mara moja wao husamehewa, wanapokelewa hata kama walifanya maovu kiasi gani.

Siku ile ilikuwa ni siku ya maandalio, yaani ijumaa, na wale wanawake waliokuja toka Galilaya kama Mariamu, walimfuata wakaliona kaburi na mwili jinsi ulivyowekwa. Wakarudi kwao wakafanya marhamu au manukato, na siku ya Sabato walistarehe kama ilivyowamriwa, wakingoja waende kuweka marhamu kwenye mwili Jumapili. Pia walisherekea siku kuu ya pasaka kama ilivyokuwa, wengi wasijue kwamba Pasaka wa Kweli, amekwisha kutolewa kama kafara, yaani Mwili wa Yesu, Mwana-Kondoo wa Mungu. Waliokuwa hekaluni waliona lile pazia lililokadiriwa kuwa na zaidi ya nchi sita kwa unene, lililovyopasuka lenyewe bila kisu, na kuacha Patakatifu pa Patakatifu paonekane wazi huku kondoo aliyekuwa madhabahuni tayari kwa kuchinjwa akikimbia. Wengine wakachunguza Maandiko zaidi ili wajiridhishe nini hasa maana ya tukio lile.

Mariamu akiwa msalabani na kwenye mazishi alikumbuka Maneno yote tokea kwenye ujauzito wa Yesu malaika alimwambia, "Roho Mtakatatifu atakujilia juu yako, na nguvu za Aliye juu zitakufunika kama kivuli, kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa Kitakatifu, Mwana wa Mungu."Yesu Ndiye pekee aliyezaliwa duniani akiwa

Mkamilifu na Mtakatifu. Ila sasa watu walimwua na Alizikwa bila hata kufanyiwa matanga. Emanueli Mungu pamoja nasi, kama alivyotabiriwa kwenye Isaya 7. Kuelewa upendo wa Yesu, mpango wa mbingu na maisha aliyoishi ya chini ili tupate wokovu, ni siri na fumbo kubwa ambalo tutaendelea kujifunza milele zote na tusifikie ukomo. Tuendelee kusoma Neno la Mungu tena na tena, na kutafakari fumbo au siri hii ya Mungu kufanyika mwanadamu na kufa kwa ajili yetu sisi wakosefu. Kitakuwa kitu cha kujifunza mbinguni milele zote.

Ndipo Mariamu akatambua zaidi Maneno yale ya nabii Simoni aliyesema "Nawe mwenyewe, upanga utaingia moyoni mwako, ili yafunuliwe mawazo ya mioyo mingi." Mariamu alikuwa amepitia mahali pengi kama Mama, na sasa hata Mume wake Yusufu alikuwa ameshafariki. Mariamu alimpoteza Yesu kwa siku tatu akiwa na miaka 12 na akafadhaika. Alipokuwa na miaka 30 watu wengi walimwambia pengine kuna shida ya mawazo kwa Mtoto Wake, kila mtu Yerusalemu alikuwa ameshamjua Yesu. Wengi walijua alikuwa hana hatia kabisa, ila walishindwa kusimama imara. Kama ilivyokuwa kwa kesi ya kifo cha Yohana mbatizaji.

Yesu alizaliwa aokoe watu kutoka katika dhambi zao, na kuvunja nguvu za dhambi kabisa kwa kutusaidia tushinde dhambi na kutupeleka mbinguni, ambapo hakuna dhambi milele zote. Ila katika haya yote, ya kufa na kuzikwa, Mariamu, alibaki katika fumbo lisilo na majibu, hadi ilipofika Jumapili ile ya ufufuo na pale Yesu alipopaa, na siku ya pentekoste wakati wanafunzi walipopokea Roho Mtakatifu na Yeye Mwenyewe akiwemo. Hapa ndiyo alielewa zaidi mambo kuliko siku za nyuma, akaweza kuyaunganisha pamoja. Nasi leo tuyaunganishe haya yote pamoja ili imani yetu kama watoto wa Mungu ikue.

Tunawafahamu watu wachache waliomwendea Yesu wakitaka kuwa wanafunzi Wake wasiweze, kwa ajili ya 'gharama'. Mfano wa mtu mmoja aliyemwendea na kusema awe mwanafunzi naye akaambiwa na Yesu sawa njoo, ila akaomba apewe muda kwenda kumzika baba yake. Huyu sijui kama alisema Ukweli maana desturi ile ya Wayahudi mtu alizikwa siku ile ile aliyokufa. Twajiuliza, huyu naye alikuwaje bado anatembea huku na kule badala ya kukaa kwenye kilio apewe pole. Mwingine alipomuomba Yesu kuwa mwanafunzi alijibiwa "Mbweha wana mashimo, na mapango na hata watu wana mahali pa kulala ila Mwana wa Adamu hana mahali pa kuweka kichwa Chake." Pengine hilo likamfanya aone ataishi maisha magumu naye akatokomea. Mwingine aliomba akaseme kwaheri kwanza ili ajipange vizuri kisha arudi. Kila mtu anapewa tiba na maagizo yake kuhusu safari ya kwenda mbinguni, safari za watu wawili hazifanani. Mungu anaangalia jinsi haiba ya mtu ilivyo na jinsi atakavyopata mafanikio zaidi katika kutembea na kufika mwisho wa safari.

Marafiki na ndugu wengine walirudi toka Golgotha au Kalvari. Nikodemu alirudi na kuwa mwanafunzi wa Yesu wazi wazi. Kumfuata Mwenyezi Mungu kuna gharama, siyo lelemama. Je waweza kumfuata Yesu bila kuona aibu, hata marafiki zao wakikucheka? Jambo moja la ajabu ni kwamba hakuna anayejua majina ya wajumbe wengine 69 kati ya wale 71 wa baraza au bunge la Wayahudi la Sanhedrini, isipokuwa hawa wawili, Yusufu na Nikodemu. Hawa wataendelea kusimuliwa

milele kwa sababu walimchagua Yesu. Mengi tunayofanya siku hizi, toka utoto mpaka ukubwa, husahaulika kabisa, ila madogo na machache tunayomfanyia Yesu hukumbukwa milele.

Kuhusiana na Yuda Iskariote, yeye alikuwa na uchaguzi. Uhuru wa kuchagua ni zawadi kutoka kwa Mungu. Kila siku sisi tunachagua. Je! Tutamchagua nani, Baraba au Yesu? Twaweza kusema kuwa Yuda anapaswa kujilaumu mwenyewe, maana katika miaka ile mitatu na nusu Yesu alimwonya tena na tena. Lakini pia tunaweza kusema Yuda alikuwa amesalitiwa na viongozi wa kanisa. Hawa waliona hatia yake ila hawakumsamehe au kumwonyesha jinsi ya kuungama.

Yesu alikuwa hana hatia na Pilato aliona fika akasema "Sioni kosa lolote Kwake." Mwanajeshi msalabani naye akasema "Hakika Mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu." Naye Yuda alisema hakika nimesaliti "damu isiyo na hatia." Viongozi wa kanisa hawakuwa na shida ya kumwua Masihi ila walikuwa na wasiwasi kuhusu pesa zenye hatia ya damu! Yuda alikuwa na majuto, na siyo toba. Alisikitikia matokeo ya dhambi ila si dhambi yenyewe, naye alijiua. Pilato alithamini wadhifa wake na maneno ya watu zaidi ya Maneno ya Masihi. Lazina tuwe waaangalifu katika shuguli zetu kama wafuasi wa Kristo, kwamba ni nani tunachagua kumpendeza. Je! Wewe unatoa tumaini la wenye dhambi na kuwaonya pia?

Ufunuo wa kushangaza ni kuwa mke wa Pilato alipewa ndoto yenye mafunuo ya kushangaza nayo ilionyesha upendo wa Mungu kwa Pilato. Mtu mmoja amesema " Kwa kujibu maombi ya Kristo, mke wa Pilato alikuwa ametembelewa na malaika kutoka mbinguni, na katika ndoto alikuwa amemwona Mwokozi na kisha aliongea Naye. Mke wa Pilato hakuwa Myahudi, lakini alipokuwa akimwangalia Yesu katika ndoto yake, hakuwa na shaka juu ya tabia Yake au misheni Yake. Alimjua na kumwona Mkuu Huyu wa mbinguni. Alimwona akishtakiwa kwenye ukumbi wa hukumu. Aliona mikono Yake ikiwa imefungwa kama mikono ya mhalifu. Alimwona Herode na askari wake wakifanya kazi yao ya kutisha. Alisikia makuhani na watawala, waliojaa wivu na uovu, wakishutumu kama wendawazimu. Alisikia maneno yote "Tuna sheria, na kwa sheria yetu anapaswa kufa." Aliona Pilato akimpa Yesu mapigo ya kuchubua, hata baada ya kutangaza, "Sioni kosa lolote Kwake." Alisikia hukumu hiyo ikitamkwa na Pilato, na akamwona akimtoa Masihi kwenda kwa wauaji Wake. Aliona msalaba ukiinuliwa juu ya Kalvari. Aliona dunia ikiwa imefungwa gizani, na akasikia kilio cha ajabu, "Imekwisha." Tukio lingine lilikutana na macho yake. Alimuona Kristo ameketi juu ya wingu kubwa jeupe, na wauaji wake wakikimbia kutoka kwenye utukufu Wake. Kwa kilio cha kutisha, mara moja mama huyu aliamka kutoka kwenye ndoto na kuandika maneno katika barua ili iende kwa mume wake Pilato kumwonya. " Hakika, Rehema na neema ziliongezwa kwa Pilato, lakini la kusikitisha ni kuwa alipuuzia mafunuo haya kutoka kwa Bwana.

Maombi yangu leo: Mpendwa Bwana, Bwana atusaidie tuwe waangalifu kila wakati kwa mafunuo ya kushangaza na yenye rehema na neema. Je! Uko pamoja nami?
Wakati Yesu alilia, "Mungu wangu, Mungu wangu, kwanini umeniacha?" (v.46), aliwasiliana na wafuasi wake wote kwamba alikuwa amelipa gharama ya mwisho kwao. Yesu aliwekeza maisha Yake ya kimwili na ya kiroho kwa ubinadamu wote.

Hakuna mtu anayeweza kuhoji upendo wa Yesu. Kujitolea Kwake kulikuwa ni kukubwa sana hivi kwamba alikufa kwaajili ya sisi sote. Je, unakata shauri leo kumtumikia Yeye maisha yako yote?

*Omba na Amini — MUNGU hasemi, Omba mara moja, nawe utapata. Yeye anatusihi tuombe. Tuendelee kuomba bila kupata uchovu. Kudumu katika maombi kunamleta mwombaji katika kujibidisha zaidi, na kumpa shauku ya dhati zaidi, na kuongeza shauku ya kupokea vitu anavyoomba. Kristo alimwambia Martha kwenye kaburi la Lazaro, "Ikiwa utaamini, utaona utukufu wa MUNGU."
-----------------------

Maswali: Ni nani alipewa mwili wa Yesu? Nikodemu alisaidia mambo gani k wenye mazishi? 'Siku ya maandalio' unajiandaa namna gani? Kwa nini Yesu hakuwa na mahali pa kulala? Twawezaje kuifanya kafara ya Yesu isipotee bure? Yusufu na Nikodemu wanatupa somo gani?

**SIKU YA 285.**
**(Oktoba 11)**

# Kufufuka kwa YESU: Habari Njema Kupita Zote Ulimwenguni!

**Marko 16**



Wanafunzi wakiwa na hofu kwamba maisha yao yako hatarini, na kwamba wamemwua Kristo sasa itakuwa zamu yao kuuawa. Wakarudi kwao na kusahau Yesu alichowaambia kitatokea. Imani yao ilikuwa imerudi nyuma sana. Hawakutafakari kuhusu Yesu, kwamba ni Masihi; na unabii wa Masihi unasema nini. Walikuwa wamechanganyikiwa kabisa maana miaka yote mitatu na nusu waliweka maisha yao yote Kwake, waliacha majumba yao na kutembea Naye kila mahali na sasa Amekufa! Wiki hiyo Yesu alikuwa amepanda punda kama 'Mfalme' na kuuawa wiki hiyo hiyo. Wakafikiri vyeo walivyogombania vimetokomea milele kabisa. Hata nasi siku ya ijumaa huja katika maisha yetu, ila jumapili ipo njiani inakuja!

Siku ya pili japo ilikuwa Sabato au siku ya mapumziko, makuhani wakiwa na hofu na huku dhamira zikiwashitaki, wale wakuu wa makuhani au wachungaji na maaskofu wakubwa walimwendea Pilato wakisema "tumekumbuka, yule Mjanja, alipokuwa akali hai, alisema atafufuka baada ya siku tatu, basi amuru kaburi likalindwe ili wanafunzi Wake wasije wakamwiba na kuwaambia watu amefufuka katika wafu." Japo walisema wamepumzika siku ya Sabato, na kujulikana na sheria zao 1521 za kutunza Sabato, bado walikuwa wakihenyeka kwenye vibarua vya uovu. Vibarua hivi walifanya maisha yao yote, Alipokuwa hai, hata walipomkamata, walipomhukumu, na hata Kumwua.

Mara zingine waliwaza "ufufuo ni kitu kinawezekana kwa Yesu kwani alifufua wengine" Pilato akawaambia, "mna askari, nendeni mkalilinde kaburi kwa kadiri ya usalama mjuao." Wakaenda kulilinda wakilitia kaburi mhuri, pamoja na wale askari wa ulinzi. Mioyoni walifikiria, kwamba japo wanasema ni Yesu ni mjanja kuweka mawazo yao shwari, Ukweli ni kwamba, walikuwa na hofu kubwa, kwani kila alilolinena Yesu lilitimia wakati anafanya huduma kati yao, kamwe hakusema uongo.

Walijua baada ya kukaa Naye, kwamba walimwamini Yeye kuliko walivyojiamini wenyewe. Yaani wao wangeweza kusema uongo ila si Yeye! Na pia alikuwa na uwezo na mamlaka ambayo hakuna binadamu mwingine aliwahi kuwa Nayo!

Lazima waliweka walinzi wengi wakifikiri hii itasaidia ulinzi wao. Hili nalo likawa jema kwa waumini, kwani walinzi hawa walikuwa wengi kutopoteza ushahidi wa ufufuo waliouona kwa macho yao. Wakati watu wote wamelala usiku ule, hakuna aliyekaa kule kaburini kushuhudia ufufuo isipokuwa wale wapinzani. Pengine hata mamia ya askari waliwekwa! Jumapili ilikuwa imefika, Mauti haikuweza kushinda, Yesu ni Ufufuo na uzima. Haleluya! Apewe sifa Mwenyezi Mungu, Ambaye ni Mweza yote; Yesu alifufuka. Habari njema ilikuja Jumapili baada ya Yesu kupumzika kaburini. Lazima tu wale walinzi waliyaona yote yaliyotokea, na hata sauti za Malaika na Yesu Mwenyewe alipofufuka, ila walipoeleza wakuu, na makuhani walipewa rushwa ili kupoteza ile Kweli, yaani waseme uongo eti, askari walilala na wanafunzi Wake waliuiba mwili.

Jambo hili watu wengi walijua si la Kweli, kwani kama walilala, walionaje wanafunzi wakiuiba mwili? Au kwa nini wale askari wasiadhibiwe kwa kulala usingizi wakiwa kazini, au kwa kuachia uhalifu kama huu utokee? Askari wale na watu wa mji ule walishuhudia tetemeko la ajabu. Ndipo Yesu alitoka kaburini. Lazima askari walimwona Yesu akitoka na mng'ao Wake ukafanya wagande. Waliona maajabu ambayo mimi na wewe tungependa tushuhudie. Mariamu na mitume walishuhudia kaburi tupu, na vitambaa au nguo zilizokunjwa vizuri. Wezi hawawezi kufanya kazi ya udobi wa nguo waibapo vitu. Kwamba wazifue nguo, wazipige pasi na kuzikunja vizuri wanapokuja kuiba mwili. Basi kwa uovu watu walilindana, badala ya kuomba toba, na kutoka kwenye mlolongo wa ulaghai wa mwovu. Uwe mwangalifu maana watu walaghai wa namna hii wapo leo pia, wanaokanusha habari za Mungu.

Mabilioni wamemwamini Yesu toka siku ile, kwa ushuhuda wa Kweli, maana penye Kweli, uongo hujitenga. Wengine kwa kule kusema damu yetu na iwe juu yetu na watoto wetu, waliishi maisha ya hofu, pengine wakafikiri watakutana na Kristo Hai njiani awaulize. Hata siku ya Sabato ilipokwisha, mapambazuko ya siku ya kwanza ya juma, yaani Jumapili, kabla ya jua kuchomoza, Mariamu Magdalenana, Mariamu yule mama wa Yakobo, Yohana na Yusufu na Salome walienda kulitazama kaburi. Walikuwa na manukato wapate kupaka mwili wa Yesu. Hawakuona mwili, nao wakafadhaika sana.

Kilichotokea usiku ni tetemeko kubwa katika nchi, kwa sababu Malaika alishuka kutoka mbinguni akaja akaliviringisha lile jiwe akalikalia. Habari njema na ya muhimu kupita zote jana, leo na kesho, Yesu amefufuka. Yeye ni Ufufuo, Kweli na Uzima. Pengine Malaika akivingirisha jiwe alimwambia Yesu "Mwana wa Mungu Baba Yako anakuita, toka nje." Mwenye uhai alikuwa amelala kaburini kwa siku tatu, akafufuka. Yesu ni ufufuo na uzima! Kwa vile Amefufuka hilo ni tumaini letu wote binadamu, kwamba tukifa tutafufuka. Kufufuka kwa Yesu ni ushindi mkubwa wa dhambi, mauti na Ibilisi. Hebu tufurahi leo!

Japo wanafunzi wa Yesu walisikitika Ijumaa, Jumapili ilipowadia wakafurahi



kupita kawaida. Malaika aliyekaa juu ya jiwe, sura Yake ilikuwa kama umeme ule unaokuja kabla ya radi, na mavazi Yake meupe kama theluji, kwa kumwogopa wale walinzi walitetemeka, wakawa kama wafu. Malaika yule alipoona wale wanawake aliwaambia wasiogope "kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulubiwa. Hayupo hapa kwani Amefufuka kama alivyosema imempasa Mwana wa Adamu kutiwa mikononi mwa wenye dhambi, na kusulibiwa na kufufka siku ya tatu." Akawaita wapatazame alipolazwa, Akawaambia waende wawaambie wanafunzi Wake "amefufuka katika wafu" na amewatangulia kwenda Galilaya ndiko mtakakomwona. Wale wanawake waliondoka upesi kutoka kaburini kwa kutetemeka, ushangao, hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi Wake.
Mtu wa kwanza kumwona Yesu baada ya ufufuo alikuwa Mariamu Magdalena, maana alirudi tena kaburini. Hakika Mungu hana upendeleo, kwani watu wangeweza kusema 'ilikuwaje mtu mwenye mapepo akawa wa kwanza kutokewa na Masihi aliyefufuka! Mungu anaangalia nia ya mtu, na upendo wake Kwake, na katika kumtii na kumtegemea Yeye. Basi Alirudi akakaa nje ya kaburi akilia "wamechukua BWANA wangu", akiwa na machozi mengi machoni aliona Malaika wawili wenye mavazi meupe wameketi mmoja kichwani na mmoja miguuni mwa lile kaburi, alimolazwa Yesu. Malaika wakamwambia "Mama unalilia nini?" akasema "kwa sababu wamememwonda Bwana wangu wala sijui walikomweka." Naye akiisha kusema haya aligeuka nyuma, akamwona Yesu amesimama, akafikiri ni mtunza makaburi. Yesu akamwuliza "mama unalilia nini? Unamtafuta nani?" Naye akafikiri mtunza bustani amechukua mwili akasema "Bwana ikiwa umemchukua wewe uniambia ulipomweka nami nitamwondoa."

Yesu akamwita "Mariamu!", Mariamu akageuka na kutambua sauti, akasema kwa furaha na kwa sauti "Raboni", yaani mwalimu wangu. Akitaka kumshika Yesu ahakikishe, nafikiri binadamu tuna udadisi wa kuhakikisha mtu akifufuka, kama

ni kweli anashikika au ni halisi. Yesu alimwambia "Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini enenda kwa ndugu Zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba Yangu Naye ni Baba yenu, kwa Mungu Wangu Naye ni Mungu wenu." Mariamu Magdalena akaenda kuwapasha wanafunzi ya kwamba "Nimemwona BWANA", akawaambia watu yaliyotokea.

Wale wanafunzi wa Yesu, ndugu na marafiki waliokuwa wanaomboleza, walipoambiwa na Mariamu, kwamba amemwona Yesu hawakusadiki; japo Yesu aliwaambia Maandiko yatakavyotimia na yote yatakavyokuwa. Walifikiri wanawake hawa wanapata ndoto za mchana masikini. Kuna ushahidi mwingi kwetu tunaomwamini Mungu kwamba Yesu anaishi tena. Alimtokea Mariamu Magdalena na Mariamu wengine wawili. Alimtokea Petro, Kleopa na mwenzake. Aliwatokea mitume kumi pamoja, na kisha 11 wakiwa pamoja. Aliwatokea saba kwenye ziwa la Tiberia. Aliwatokea watu 500 Galilaya akipaa na walimwona kutoka na 1 Korintho 5:6. Alimtokea Yakobo Yerusalemu, na wengi aliporudi mbinguni, kama vile Paulo kwenye njia ya Damesiki.

Hata Stefano wakati anauwawa alimwona Yesu mbinguni. Na Paulo alimwona Kwenye hekalu, kisha Yohana kwenye kisiwa cha Patmo. Hawa waliwashuhudia wengine, Yesu Yu hai leo. Wale wasio Wakristo nao walishuhudia kwani walimwona pia, haya yameandikwa miaka michache baadaye na wanahistoria, wakieleza waliyosema watu waliomwona Yesu akiwa anaishi tena baada ya ufufuo. Mambo yote haya yameandikiwa ili tujue na kuamini kwamba YESU YU HAI LEO! Endapo Yesu Mwokozi wetu angekufa bila kufufuka, habari njema isingekuwa timilifu. Kufa Kwake ni ushindi kwetu, na kufufuka Kwake ni ushindi kwetu pia. Yesu Yupo mbinguni mkono wa kuume wa BABA. Mkono wa kuume unaonyesha mamlaka Yesu aliyo nayo.

*Kuna nguvu inayotakiwa kupatikana kutoka kwa MUNGU. Yeye ana uwezo wa kusaidia. Anaweza kutoa neema na hekima ya mbinguni. Kama utaomba kwa imani, utapokea; lakini ni lazima ukeshe katika maombi. Kesha, omba, fanya kazi, inapaswa kuwa kauli mbiu yako.


---------------------------

Maswali: Kwa nini waliweka walinzi kwenye kaburi? Kwa nini unafikiri walinzi walichosema kilikuwa uongo? Malaika alisemaje alipoona wale wanawake? Tunajuaje kwamba Yesu yu hai leo? Moja wapo ya kazi Zake Yesu mbinguni ni nini leo kutokana na kitabu cha Waebrania?

**SIKU YA 286.**
**(Oktoba 12)**

# Njia ya Emmaus: Kleopa na Mwenzake wapata masomo ya Biblia!

**Luka 24**



Siku ile ya Jumapili, baada ya Mariamu kumwona, watu wawili waliomwamini Yesu walikuwa wakienda kijiji kimoja kiitwacho Emau; ambacho kilikuwa umbali wa kutembea masaa mawili au km 12 hivi. Hawa walikuwa wamekata tamaa kwani matumaini yao yalikatishwa. Watu hawa walikuwa wanazungumzia na kuulizana mambo yaliyotokea. Walikuwa wamesikia kwamba mwili wa Yesu umepotea na wanawake wameonana na Malaika na kuzungumza nao. Hizi ndizo zilikuwa 'taarifa za habari, na magazeti' au mambo yaliyotawala mazungumzo juma lile, yakiwapa huzuni na kuwakatisha tamaa.

Wengine walikuwa wamepotoshwa na nadharia za masadukayo kwamba hakuna ufufuo, na badala ya furaha kwamba Yesu sasa Yupo mbinguni, amefufuka wao wakahuzunika. Naye Yesu alikuwa nyuma yao, kisha alikaribia na wakamkaribisha kwenye mazungumzo na kuandamana nao. Macho yao yalifumbwa yasimtambue,

kwa sababu ya huzuni ile kuu waliyokuwa nayo na hata machozi, yaliwafanya wasifikiri kwa wazi. Naye Yesu akawauliza "Ni maneno gani haya mnayosemezana hivi mnapotembea?" Wakasimama wamekunja nyuso zao kwa huzuni, kisha mmojawapo aitwaye Kleopa akajibu "Je Wewe ni mgeni hapa Yerusalemu? Maana itakuwa ni Wewe tu usiyejua yaliyotokea siku hizi chache zilizopita?"

Yesu akauliza, ni mambo gani yametokea? Wakamwambia mambo ya Yesu mnazareti, aliyekuwa nabii mkubwa na mtu Mwenye uwezo wa kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote vyema. Wakamwelezea jinsi "wakuu wa makuhani, na wakubwa walivyomtia katika hukumu na kumsulubisha, nasi tulikuwa tukimtumaini ya kuwa Yeye Ndiye atakayewakomboa Israeli kutokana na makucha ya utawala wa Rumi. Zaidi ya hayo, leo ni siku ya tatu, tangu yalipotendekea hayo mambo, tena wanawake kadhaa wa kwetu walitushtua walipokwenda kaburini mapema, wasiuone mwili Wake; wakaja wakisema ya kwamba wametokewa na Malaika, waliosema kwamba Yu hai. Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikwenda kaburini wakaona vivyo hivyo kama wale wanawake walivyosema, ila Yeye hawakumwona."

Yesu aliwasikitikia kwa huzuni zao, maana alijua hawa walikuwa wanafunzi Wake waliompenda, ila walipotoshwa na mapokeo aliwaelezea vyema haya ila hawakuamini. Akawambia kwa upendo "Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyosema manabii, Je haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu Wake?" Wakashangaa mbona mgeni huyu ana maneno ya mkazo vile? Akaanza kurudi nyuma na kuanza kuwasimulia historia ya kutoka kwa Musa na manabii wote, akawaeleza katika Maandiko yote mambo yaliyomhusu Yeye Mwenyewe.

Akawaeleza yote hata kufa na kufufuka siku ya tatu na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa Jina Lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanzia Yerusalemu, nao ndiyo watakuwa mashahidi Wake. Akawaambia yahusuyo kuvikwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu utokao juu. Nafikiri hata nasi tungependa kuwa na mafundisho matamu ya Biblia kama hayo ambayo Kleopa na mwenzake walipata. Hata leo ni muhimu kutumia unabii wa Agano la Kale kujua Yesu ni Masihi, na kielelezo chetu. Kifo Chake pia ni shuhuda kubwa ya kwamba Ndiye Masihi aliyetabiriwa.

Watu wengi siku hizi hawatumii Agano la Kale. Hili ni kosa kubwa, kwani Agano la Kale linatusaidia kuelewa Agano Jipya kwa ubora zaidi. Agano jipya ni mwendelezo wa Agano la Kale. Hawa ni mapacha wasioweza kutenganishwa. Agano la Kale linazungumzia uumbaji kwenye sura ya kwanza na ya pili, na sura ya tatu kuanguka dhambini kwa mwanadamu na mwanzo wa kuzungumzia kuhusu kuja kwa Masihi kutuokoa kutoka dhambini. Na Sura 1186 zilizobakia zinaendelea kuzungumzia kuhusu wokovu wa mwanadamu. Agano la Kale ni Neno la Mungu, pumzi Yake na Maneno Yake yenye mamlaka ya mwisho. Wayahudi wengi nao hawamwamini Yesu au Agano Jipya, nayo hii ni shida kubwa, maana Yote ni muhimu katika safari yetu ili kupata picha kamili.

Nilifanya kazi na Wayahudi kwenye Hospitali yao karibu na Jiji la New York, nikakuta wengi wanatumia Agano Jipya na hadithi za mapokeo kama Talmud kuwa msingi wa imani. Wengine walichukua hadithi hizi za mapokeo, nao wakaacha kabisa hata lile Agano lao la kale. Kutoa mamlaka kwa mapokeo, au madhehebu kuliko Biblia, si kosa tu bali ni dhambi. Niliona Wayahudi hawa tukizungumza, wengine walitoka kwenye mstari kabisa wa mpango wa Mungu na Neno Lake, japo walikuwa Marabi au walimu wa dhehebu lao. Tunapaswa kuweka tahadhari ya hilo maana ndiyo udhaifu wetu wanadamu wote.

Neno la Mungu si Maneno mazuri tu tunayoweza kuyafuata tukitaka au kuchukua haya na kuacha yale, bali ni mamlaka ya mwisho mbinguni na duniani. Naye Mungu hujifunua kwa watu kuhusu hili hatua kwa hatua. Hatua za watu hutofautiana. Agano la Kale na Jipya yanategemeana, usiposhika moja, uwezekano wa kuwa umeyavunja yote ni mkubwa. Yawezekana mtu asiwe na Maandiko yote, kama rafiki Yangu Msafiri Mtenzi, mmishonari wa Tanzania kule Kongo Kisangani, alikuta watu wana vipande vya Biblia, wengine vitabu vya Musa, wengine barua za Paulo n.k. Kesi ya aina hii ni tofauti, kwani wana kile walicho nacho na kukisoma na kukifuata. Si wote walio na Biblia nzima. Hiyo inatokana na sababu mbalimbali. Hadi sasa Biblia yenyewe imeweza kutafsiriwa kwa lugha 2900 tu, na kama lugha 1680 zinahitaji tafsiri kwani kunahitajika nyenzo nyingi kama vile kujua lugha na kupata fedha za kutafsiri na kuchapa (Watafsiri wa Biblia wa Wycliffe).

Basi kisa chetu kinaendelea kikisema, wakina Kleopa wakakaribia kile kijiji walichokua wakienda Naye Yesu, akafanya kama anataka kuendelea mbele. Wakamshawishi wakisema, kaa pamoja nasi, kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha, na ni hatari kutembea usiku. Desturi yao ilikuwa ya kuwapenda na kuwakarimu wageni, hasa huyu ambaye mpaka hapo lazima walikuwa wameona tofauti kubwa katika kuzungumza Kwake. Basi akaingia ndani na kukaa nao, wakamtayarishia chakula, Naye akiwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate akaubariki, akaumega na kuwapa. Ndipo yalifumbuliwa macho yao, wakamtambua Yeye ni nani!; Naye alitoweka pale pale mbele ya macho yao, nao wakaambiana, ndiyo maana masomo ya Biblia aliyotupa yalikuwa ya ajabu! “Mioyo yetu iliwaka ndani yetu alipokuwa akisema nasi njiani na kutufunulia Maandiko.”

Wasingemsisitiza akae nao wasingebarikiwa vile. Yesu hamlazimishi mtu aingine ndani ya nyumba au moyo wake. Huingia nyumba ya masikini au tajiri yoyote kwa ruhusa, kisha anajaza mioyo yetu furaha na amani tele ambayo inaleta ladha ya maisha. Hebu tusijifanye tuna shughuli na kushindwa kupokea wageni leo, bali tuonje na kujua jinsi BWANA alivyo. Wengi wamekaribisha malaika kwa kuwa wakarimu. Wale wakina Kleopa safarini Emau nao wakaondoka sasa usiku ule ule wakirudi Yerusalemu, wasijali uchovu au njaa yao, maana walikuwa wamepata nishati na furaha mpya.

Hakukuwa na taa njiani, pengine walijikwaa hapa na pale, lakini hawakujali walikuwa na msisimko wa furaha kuu. Wakawakuta wale 11 wamekutanika wote na wale waliokuwa pamoja nao, wakasema BWANA amefufuka kweli kweli, Naye akamtokea Simoni Petro. Sasa walikuwa wanasimuliana wakiwa na matumaini mapya ya

dhati. Wakawaeleza kwamba kufa kwa Masihi kwa njia ya ukatili kumetimiza unabii. Masihi asingekuja kama Mfalme kwanza, kama wengine wafikiriavyo. Wakaawambia wafuasi jinsi kifo kile kinavyowaokoa. Nao wakina Kleopa waliwapa habari ya Mambo yale ya njiani Emau na jinsi Yesu alivyotambulikana nao katika kuumega mkate. Wakafurahi wakisema "YESU Anaishi."

Walipokuwa wakizungumza tazama Yesu akaingia na kusimama katikati yao, akawaambia, "amani iwe kwenu." Wakashtuka na kuogopa wakifiriki ni roho au mzuka. Kwani milango ilikuwa imefungwa! Wakisahau kwamba ana Uwezo usio wa kawaida! Akawaambia mbona mnafadhaika na kuona shaka mioyoni mwenu? Ndipo alipowaomba wamguse ili kuthibitisha kama ni Yeye.

Kuna maswali matatu muhimu sana maishani: 1.) Ninatoka wapi? 2.) Kwa nini niko hapa? 3.) Ninaenda wapi? Kwa Mkristo, Mwito ule wetu Mkuu wa "Enendeni ulimwenguni kote" unatoa jibu la swali la pili: tuko hapa wakati huu wa mwisho, kutumiwa na Mungu kuutayarisha ulimwengu kwa ajili ya wakati mwisho kwa kuhubiri injili. Maisha yana maana tu tunapojitolea kwa kazi hii! Ili kuwa na ufanisi katika kuishinda nafsi, kumbuka hili: Njia ya Kristo pekee ndiyo itatoa mafanikio ya kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alichangamana na wanadamu kama Yule ambaye aliwatakia mema. Alionyesha huruma Yake kwao, aliwahudumia mahitaji yao, na akapata ujasiri wao. Kisha Akawaambia, 'Nifuateni Mimi!'

*Ikiwa utapata sauti na wakati wa kuomba, MUNGU Naye atapata wakati na sauti ya kujibu.

---------------------------

Maswali: Watu wawili walikuwa wakienda kijiji gani? Kwa nini nyuso zao zilikuwa na huzuni? Yesu aliwafariji kwa Maneno gani? Je, moyo wako umeshawahi kuwaka kwa kusikia Neno la Mungu? Walijuaje kwamba ni Yesu aliyekaa nao? Kleopa na mwenzake walifanya nini Yesu alipotoweka? Je, una mpango gani wa kujifunza Maandiko ili uelewe unabii na kinachoendelea leo? Je, twawezaje kufumbuliwa macho leo kama wanafunzi wa Emau?

**SIKU YA 287.**
**(Oktoba 13)**

# Simoni na Yohana wanaenda kaburini kuhakikisha.

**Yohana 21, Luka 24**

"Yesu amefufuka" ndizo zilikuwa habari kila mahali. Habari za kaburi lililokuwa tupu ziliendelea na mamilioni, au pengine Wayahudi wote walisikia. Haikuwa siri tena. Maana watakatifu walifufuka Naye toka makaburini na wakawatokea watu. Yesu aliposema imekishwa, pambano lilikuwa limekwisha, na mbingu ikashangilia ushindi, na Shetani akawa ameshindwa. Binadamu, viumbe vyote, na hata Malaika wakaelewa mpango wa wokovu kuliko hata hapo mwanzo, kwani wenzao wengine walimfuata Shetani kwa kutojua, ila baada ya Mungu kuonyesha upendo Wake kwetu sisi wakajua kwamba Uwezo na Nguvu za Mungu zinatokana na wema, huruma na upendo Wake. Wote wakakiri Mungu ni wa Kweli na wa haki.

Kwa miaka 4,000 Shetani alikuwa amefanya kazi ya kumdidimiza mwanadamu ila Yesu alifanya kazi kumnyanyua. Kutoka Yesu alipozaliwa Shetani alijaribu kupinga mpango wa wokovu kwa kufanya mambo yaende kombo (mrama) ila sasa alikuwa ameshindwa. Shetani ambaye anajua upendo, rehema na wema wa Mungu kuliko hata wanadamu, alidanganya wengi kwamba Sheria ya Mungu si ya upendo na kwamba haiwezi kutiiwa, ila baada ya kifo cha Yesu shitaka hili lilikwisha. Alikuwa amepoteza nafasi yake ya kutubu, mlango wake wa rehema ulikuwa umefungwa, alikuwa amekataa katakata kutubu. Shetani aliamua kuwa mwasi hakuna aliyemdanganya yeye, bali binadamu alikuwa amedanganywa na Shetani, na Mungu kwa huruma Yake, japo tulikuwa hatuna udhuru alitutoa kwenye adhabu hiyo kali.

Leo hii tunapopewa nafasi ya kujua injili, tunakuwa hatuna udhuru, kwani tunajua upendo wa Mungu ulivyo mkuu. Mungu anatoa rehema kwetu sote, na anajua pale ambapo mtu amekataa katakata kuipokea injili, wakati imetambulishwa kwake. Yeye hutukirimia zawadi kuu na uwezo wa kuishi maisha ya utakatifu kwa neema Yake. Huruma, Kweli na haki vimeelezwa vizuri kwa kifo Chake kwamba vinapaswa kuwa kwenye kifurushi kimoja, kwa maana kwamba huwezi kuvitenganisha. Pambano kati ya Mungu na Shetani linaendelea mpaka mwisho wa wakati. Kila mtu, mtoto au mtu mzima anapaswa kuchagua kati ya Neno la Mungu na ahadi Zake, au Neno Lake ambalo ameliweka juu, hata zaidi ya Jina Lake.

Siku zile chache wengi walikuwa wamesikia kuhusu ufufuo wa Yesu, maana hata watu waliofufuliwa waliwatokea wengi, wakisema habari hizi njema kabla ya kutwaliwa kwenda mbinguni kama limbuko au matunda ya kwanza pamoja na Yesu. Biblia haisemi mengi kuhusu watu hawa, ila tunajua waliwatokea wengi. Mauti imeitwa kama usingizi katika Biblia. Wengi siku ile Yesu atakapokuja watasikia sauti ya

Mwana-Adamu ikiwaita kutoka katika usingizi wa mauti. Sauti isemayo "imekwisha" itapenya makaburini na wafu watatoka. Wale waliomwamini Yesu makaburi yao yatafunuliwa na watainuliwa na ile ile nguvu iliyomfufua Yesu kutoka kuzimu.
Basi Simoni Petro na Yohana walipiga mbio kaburini kuona kama mambo haya ni Kweli. Yohana ambaye alikuwa kijana alimpita mzee Petro na kuwahi kufika kaburini. Akainama na kuona vitambaa vya sanda, ila hakuingia. Petro alipokuja anahema kwa kukimbia aliingia moja kwa moja kwenye kaburi na akavitazama vitambaa na akaona leso Yake ya kichwani, haikulala na vitambaa bali imezongwa zongwa mbali mahali pa peke yake. Yohana naye akaingia kaburini, akaona na kuamini, walikuwa hawako kwenye ufahamu wao bado kwamba Imempasa Yesu kufufuka. Yale maneno 'nitawaona tena', ya Yohana yaliwapiga chenga. Basi wale wanafunzi wawili wakaenda zao nyumbani. Ndipo jioni yake, aliwatokea watu wawili Emau, wakitembea kwenda shambani, hawa waliwaambia wengine ila watu hawakusadiki. Yesu alitokea watu mara 11 hivi kwa mujibu wa maelezo ya Maandiko ya injili na barua za Paulo, katika zile siku 40 alizoishi duniani baada ya ufufuo.

Yesu alikutana na wanafunzi usiku ule wa jumapili. Japo mlango ulikuwa umefungwa aliingia, maana Yeye ana uwezo wa kwenda kinyume na asili akasema "Salamu! Amani iwe kwenu." Yesu alikuwa na makovu sita ya kusulubishwa, mawili ya miguu, na mawili ya mikono yalikuwa ya misumari, moja la ubavu lilikuwa la kuchomwa na mkuki, na moja la kichwani la ile taji ya miiba. Akawaonyesha ubavu Wake. Wakakaribia wakafadhaika wakifikiri wanaona mzuka au roho ambayo hawawezi kuishika, ila wakamshika miguu akashikika, na wakamsujudia." Wakatambua sauti ni Yake, mwonekano na jinsi anavyofanya vitu pia ulikuwa ni Wake.

Ni Neno la kuaminiwa kwamba Yesu atakapokuja tutawatambua wapendwa wetu wote waliofufuka, tutajua huyu ni Rehema, Faraja, Baraka au Tumaini. Tutaonana uso kwa uso hakika, haitakuwa roho kwa roho. Mbinguni si hali bali ni mahali halisi, ambapo watu wataishi, na kujuana. Ukimgusa mtu atagusika, hatakuwa roho, bali mtu kamili na halisia. Nilipokuwa mtoto wengine walifundisha "tutakuwa roho mbinguni, na roho zetu zitakuwa zinaelea angani zikipiga vinubi kwa furaha." Japo Biblia ipo wazi mbinguni patakavyokuwa, ila Ukweli unabaki kuwa "mengine sikio wala macho hayakuweza kuyaona hapa duniani bali yataonekana huko". Wengine hawana mipaka na hujaribu kusema kile Maandiko yasichokisema. Maandiko yanasema mbinguni ni mahali halisi. Biblia inaposema mtu, au nafsi hai, haitenganishi roho na mwili. Ili mtu awe mtu, lazima roho na mwili viwe pamoja, haviwezi kutengana kamwe, vikitengana, mtu anakuwa amepoteza maisha, amepoteza uhai.

Mwili (udongo) + Pumzi ya Uhai toka kwa Mungu= Mwanadamu au Nafsi hai
Mitume walikuwa na mengi ya kushuhudia watu, maisha Yake, kifo Kwake. Kisha Yesu akawaambia "msiogope enendeni mkawaambie ndugu Zangu, waende Galilaya ndiko watakaoniona." Yesu aliwakemea kwa kutoamini kwao, na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakusadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu. Akasema mbona mnafadhaika? Tazameni mikono Yangu na miguu Yangu ya kuwa Mimi Ndiye Mwenyewe, niguseni guseni mwone kama ni roho bila mwili au mifupa. Na baada ya kusema hayo Aliwaonyesha mikono na miguu Yake. Bado wakistaajabu

na kutoamini kwa furaha, aliwaambia “mna chakula chochote hapa?” Wakampa kipande cha samaki cha kuokwa, Akakitwaa na kula mbele yao, kuonyesha roho haiwezi kula chakula. Tunaona kwamba aliwatokea marafiki Zake kabla ya ndugu Zake, japokuwa marafiki wengine walikuwa ndugu!

Hili ni jambo tuliloshangaa pia. Tulifikiri Yesu akifufuka atawatokea ndugu Zake kwanza, na hata Malaika aliwaambia kwanza kuhusu kukutana na mitume. Nilifikiri atapeleka ujumbe kwa ndugu Zake, bali Malaika alipeleka ujumbe kwa wanafunzi na marafiki Zake kwanza, na wapendwa wengine waliokuwa wamemkubali na kumfuata, kama Mariamu na wale wanawake. Yesu pekee Ndiye mwenye uwezo wa kutoa uhai Wake na kuutwaa tena. Yeye ni Ufufuo na Uzima. Kwa vile Yesu alifufuka, tunatumaini kuwa hata nasi pia tutafufuka. Yeye ni Mfano wa wote watakaofufuliwa, yaani wale waliokufa wakimwamini Yesu, siku ile ya ufufuo wa kwanza wa asubuhi njema.

YESU ALIJIONYESHA

Wakati mwingine inaweza kuonekana kana kwamba kumjua Kristo ni jambo lisilowezekana. Lakini katika Maandiko hatupati hisia hiyo hata kidogo. Tunasoma kwamba , “Baada ya hayo Yesu akajidhihirisha tena kwa wanafunzi Wake…”Yohana 21:1. Hapa haionekani kama alikuwa Mtu anayetaka asijulikane alipo; Aliendelea kujitokeza “tena.” Maandiko yanazungumza juu ya wanawake walioenda kuutafuta mwili wa Kristo, pia yanazungumza juu ya Petro na Yohana ambao walikwenda kumtafuta pia. Lakini inaonekana kwamba Yesu alifanya mengi zaidi ili kujionyesha Mwenyewe kuliko wafuasi Wake walivyofanya ili kumpata.

1. Alijionyesha kwa Mariamu bustanini - Yohana 20:11-18
2. Kwa wanawake wengine - Mt. 28:8-10
3. Aliwatokea wanafunzi wawili walipokuwa wakisafiri kwenda Emau - Luka 24:13-32
4. Kwa Petro - Luka 24:34
5. Wanafunzi (bila Tomaso) - Luka 24:36.
6. Wanafunzi (pamoja na Tomaso) – Yohana 20:26-29.
7. Wanafunzi walipokuwa wakihangaika baharini - Yohana 21:1, 2.

Unapata hisia kwamba Yesu Yuko tayari zaidi kupatikana kuliko sisi tunavyojitahidi kumpata, “Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa mioyo yenu yote.” Yer. 29:13. Hebu tuwe macho wakati Yesu anapotokea. Inaweza kuwa kazini, au nyumbani tunapopata kifungua kinywa, au kwenye shughuli nyingine kana kwamba tunasafiri kwenda Emau.

*Ikiwa utapata sauti na wakati wa kuomba, MUNGU Naye atapata wakati na sauti ya kujibu

----------------------

Maswali: Ni nani pekee Mwenye uwezo wa ufufuo na uzima? Kwa nini Yesu aliwakemea mitume? Yesu alipitaje kwenye mlango? Kwa nini Yesu aliwaonyesha ubavu Wake? Je, ungekuwa mwanafunzi wa Yesu ungefanyaje siku ile? Japo Yesu aliwaambia tena na tena wanafunzi Wake atafufuka, kwa nini hawakuamini?

**SIKU YA 288.**
**(Oktoba 14)**

# Yesu awatokea wanafunzi Wake kwa siku 40.

**Mathayo 28, Matendo 1, Yohana 21.**



Nao wale wanawake wakienda kuwapasha ndugu za Yesu, walikutana na baadhi ya askari wakiingia mjini kuwapasha wakuu wa makuhani habari ya mambo yote yaliyotendeka. Askari walijaliwa kushuhudia tukio la ajabu la Yesu kufufuka. Wale wakuu wa makuhani wakakusanyika pamoja na wazee kufanya shauri, wakawapa askari fedha nyingi kama rushwa ya kuwaziba mdomo ili wasiseme walivyoona ufufuo. Wakawaambia "semeni kwamba wanafunzi Wake walikuja na kuiba mwili Wake, sisi tulipokuwa tumelala."

Ilikuwa ni uongo wa ajabu, kwani hata wanafunzi wenyewe hawakujua amefufuka, walikuwa na huzuni bado. Wezi kwa kawaida hawashughuliki kufanya kazi ya udobi ya kukunja nguo! Hapa kwa Yesu baada ya kufufuka nguo zilikutwa zimekunjwa vizuri! Hata hivyo wanafunzi wa Yesu wasingemdhililisha Rabi wao kwa kuiba mwili Wake bila kumvika nguo Zake. Hata hivyo mitume wote isipokuwa Yohana walikuwa tayari kufa kwa ajili ya Yesu, kama ingekuwa ni porojo, wasingetoa maisha yao vile.

Nafikiri askari walishuhudia mambo ya ajabu ya ufufuo, kabla ya binadamu yoyote na wakawaelezea makuhani matukio waliyoona. Makuhani wakawaambia watoe sababu kwamba walilala, wakastuka mwili umeibiwa. Wakawaambia walinzi watazungumza na mkuu, ili wasihesabiwe hatia kwa kulala usingizi kibaruani, maana wangepewa hatia ya kulala kibaruani wasingekuwa tayari kusema uongo ule wa kwamba Yesu hakufufuka bali mwili uliibiwa. Basi uongo huu wa wakuu wa makuhani, ulienea katika Wayahudi hata leo. Nafikiri si Uyahudi tu, bali hata dunia nzima kejeli hii ilienezwa. Wengine hawaamini kwamba Yesu alifufuka, bali ni jambo la Kweli na la uhakika, Yesu amefufuka. Watu waliona haya kwa macho yao. Mamilioni ya watu hutembelea Yerusalemu kuona hili kaburi tupu kila mwaka.

Wale wanafunzi 11 waliobakia walienda Galilaya umbali wa kilomita 120 hivi kwenye mlima Yesu alioagiza. Nao walipomwona walimsujudia, lakini baadhi walikuwa na mashaka bado, kama ni huyu Yesu mwalimu wao, waliyeishi Naye miaka mitatu na nusu au la. Yesu hakuishi nao kama awali, masaa yote, bali alikuja kuwatembelea kwa muda na kwenda. Sasa angeweza kuwa mahali popote kwenye Milki Yake kubwa isiyo na ukomo. Alizungumza nao kwa undani na wakaelewa kwamba hakuja kuleta ufalme wa dunia na siasa bali ufalme wa mbinguni, wa kiroho.

Akawaambia waanzie kazi Yerusalemu, japo watu mule walikuwa wagumu, na watesi. Hata hivyo ilikuwa nafasi yao kuungama na uovu waliokuwa wameshaufanya, walipewa nafasi nyingine kutubu kwa kuumiza watenda kazi wa Mungu. Mungu angewatendea miujiza, na ishara; na si wao tu bali wafuasi wote wanaotenda kazi Yake, mpaka mwisho wa dunia. Yesu aliwapa wanafunzi Wake karama za mambo makubwa japo walionekana hawakwenda shule. Uwezo wao ulikuwa mkubwa sana, kulinganisha na wale wenye elimu kubwa. Hata leo ni kazi yetu kuwaambia watu habari njema, watu wengi au mtu mmoja mmoja.

Wengi wana mizigo ya umasikini, mawazo, na dhamira kuwashitaki kwa ajili ya kufungwa na mwovu. Tuombe Mungu atupe upendo mwingi na wa Kweli kwao. Kwani Upendo wa Kweli usio wa kinafiki, sisi binadamu wote hatuna ila tunaupokea kutoka Kwake. Tuanze na wale wa nyumbani mwetu kwa kuwapa mkate wa uzima, kisha kwa majirani, na marafiki na hatimaye wale wasiomjua Mungu. Kama tukifanya sehemu yetu kwa imani Mungu atatenda makuu. Yesu alikuja kuponya wagonjwa na kufungua minyororo ya Shetani. Imani, yaani kumwamini ni muhimu sana, ili tufanye kazi na Mungu, katika kufikia wengine. Nafikiri malaika wanashangaa kwamba mbona hatuombi vya kutosha wakati Mungu Yupo tayari kutufanyia makubwa, na alishuka na kuacha vyote mbinguni kwa ajili yetu.

Tumeona Yesu alijidhihirisha kwa wanafunzi Wake mara kadhaa kwenye Maandiko; ila Maandiko yameandikwa kwa muhtasari. Yesu alikuwa amerudi kwenye cheo Chake cha mtawala wa mbingu na nchi. Hakukaa nao masaa 24 kama zamani. Siku moja aliwatokezea mitume kwa namna hii; Simoni Petro, Tomaso aitwaye pacha, Nathanieli, wana wa Zebedayo na mitume wengine wawili walikuwa pamoja na Simoni Petro. Simoni Petro akiwa hajui afanye nini kwa mambo mengi yaliyotokea, akawaambia wenzake "Naenda kuvua samaki", kwani walihitaji kula na ndiyo stadi aliyoijua toka ujana. Isitoshe hakujua kama atarudia kazi hii baada ya kuiacha.

Basi walienda na mitume wengine kwani baada ya Yesu kufa, walikuwa wameacha shughuli zao za kwenda Naye hapa na pale kuhubiri. Isitoshe, ilikuwa haijaingia akilini mwao kuwa kwa sasa wafanye nini. Basi waliondoka na kupanda chombo, ila usiku ule hawakupata kitu. Hata kulipokucha Yesu alikuwa amesimama ufukoni, walakini wanafunzi hawakujua ya kuwa ni Yesu. Yesu akawaambia "Wanangu mna kitoweo?" Wakamjibu la, maana hawakupata kitu, basi Akawaambia watupe jarife au nyavu tena upande wa kuume wa chombo "nanyi mtapata." Walifikiri ni nani Huyu anatuamrisha hivi, ila walitii amri wakatupa kwa sababu wasingepoteza kitu kuwa wema kwa mgeni. Walipofanya vile, wala hawakuweza kulivuta jarife tena kwa sababu ya wingi wa samaki.

Basi Yohana aligundua mapema akamfahamisha Petro "Ndiye BWANA." Simoni Petro aliposikia ya kwamba ni BWANA alijifunga vazi lake maana alikuwa tupu au na nguo chache tu akivua ili asilowe na maji. Basi Simoni alijitupa baharini nao, wanafunzi wengine wakaja na mashua maana walikuwa mbali kwenye nchi kavu, yapata kama futi 300 hivi, wakalikokota jarife na samaki wakiwa wamejaa pomoni. Waliposhuka pwani wakaona moto wa makaa na juu yake samaki wanaokwa na mkate. Yesu akawaambia walete baadhi ya samaki mliowavua sasa hivi. Petro akaenda kuleta, na japo nyavu ilijaa halikupasuka. Wakasikia harufu ya chakula kwa mbali, samaki wa kuoka! Yesu akawaokea samaki mitume na kuwaambia waje wale kifungua kinywa. Walipikiwa na Bwana, alikuwa Mpishi au Chef wao Mkuu! hata leo tusipuuzie kazi, kwamba mimi ni mvulana au msichana, kama Bwana alipika, sisi Je? Ikibidi upike, pika, na kila mtu anapaswa kujua jinsi ya kupika chakula rahisi, kisichokobolewa, au kusindikwa, ila chenye ladha nzuri, kila kijana anapaswa kujua stadi ya mapishi. Mtu asifike miaka 15 kabla hajajua jinsi ya kupika mapishi yenye afya, ladha, gharama nafuu, na yenye vyakula vinavyopatikana pale anapoishi.
Hata leo anatukaribisha tufungue kinywa kwa kusoma Neno Lake kila asubuhi. Ni hakika kuwa mitume walikuwa na bahati au baraka iliyoje kuwa na BWANA kati yao, na ni BWANA wa upendo. Hakuna kati yao aliyethubutu kumwuliza Wewe ni nani, maana wote walijua ni BWANA. Yesu akaenda akatwaa mkate na samaki na kuwapa. Hii ilikuwa mara ya tatu Yesu kuonekana na wanafunzi Wake.

*Uhitaji wetu wenyewe ni hoja kubwa tosha na inasihi kwa umbuji zaidi kwa niaba yetu. Lakini Bwana anapaswa kutafutwa ili atufanyie mambo haya. "Ombeni, nanyi mtapewa." Yeye ambaye hakumhurumia hata Mwanae wa pekee, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote. Ikiwa amefanya hivyo, je, atakosaje kutukirimia mema yote pia? Mathayo 7: 7; Warumi 8:32.
-------------------------

Maswali: Yesu alikaa na wanafunzi siku ngapi kabla ya kupaa? Makuhani walikula njama gani? Je, kula njama kunatokea makanisani siku hizi? Je, tunawezaje kujiepusha na njama makanisani? Kwa nini Yesu aliwapikia mitume? Mitume walivua samaki wangapi? Je, mara nyingine umefikiria kurudi kuvua samaki na uache kumtumika Mungu kama mitume?

**SIKU YA 289.**
**(Oktoba 15)**

# Yesu amwimarisha Petro.

**Yohana 21.**



Kwa vile Petro alimkana Yesu wazi wazi, ilikuwa muhimu amsaidie kujenga imani yake, ili akipatikana na majaribu aweze kustahimili. Petro alimpenda Yesu na alikuwa radhi kufa kwa ajili Yake, bali alizitumainia nguvu zake. Alikuwa na huzuni moyoni baada ya kumkana Yesu siku hizi tatu. Wote twapaswa kumwomba Mungu ili tuweze kustahimili majaribu. Hakuna awezaye kushinda majaribu, Mungu Ndiye anayetupa nguvu. Yesu alimwita Petro kwa jina lake ili kumpa faraja kwamba amesamehewa kabisa.

Basi walipokwisha kula samaki na mikate ambayo Yesu aliwatayarishia mitume pale kwenye bahari ya Tiberia, Yesu alimwambia Simoni Petro "Simoni wa Yohana, wewe wanipenda kuliko hawa?" Simoni akajibu "Naam BWANA Wewe wajua kuwa nakupenda." Akamwambia "Lisha wana-kondoo Wangu." Akamwambia tena mara ya pili "Simoni wa Yohana wanipenda?" Petro akajibu "Ndiyo Bwana, Wewe wajua kuwa nakupenda." Akamwambia "Chunga kondoo Wangu." Akamwambia mara ya tatu "Simoni wa Yohana wanipenda? Petro alihuzunika kusikia anaulizwa mara ya tatu "wanipenda", akamjibu BWANA, sasa akijua kwamba Mungu ajua yote, na asitegemee nguvu zake kufikiri kwamba anaweza kusimama mwenyewe bila uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Akasema "Bwana, Wewe wajua yote; Wewe umetambua ya kuwa nakupenda." Yesu akamwambia "Lisha kondoo Zangu." Alikuwa amemkana Yesu mara tatu, na Yesu alimwuliza swali hili mara tatu. Lugha ya kulisha kondoo hapa inasema ni kondoo wadogo au watoto. Hata wale wanapompokea Yesu kwa mara ya kwanza wachanga kwa imani, ni watoto wadogo. Hawa watu wazima wanaokuja kwa Yesu kwa mara ya kwanza ni kondoo wadogo pia, na wote wanakua kama watoto wadogo wanaohitaji kulishwa. Petro alijua amesamehewa, na Yesu alimwamini alishe kondoo Zake.

Uwezo wote wa Yesu uko kwa wote ambao wako tayari kulisha kondoo Zake kwa kuwaambia Maneno ya uzima bila kubagua kama ni mtoto au mkubwa. Hata leo watenda kazi wa shamba la Mungu wanaporudi nyuma na kukosa, wanapaswa kusaidiwa wajirudi, ili wasamehewe. Mungu hufanya miujiza mingi kwa wote ambao wanafanya vile.

Yesu akamwambia Petro "wakati ulipokuwa kijana ulikuwa ukiamka na kujitayarisha au kujishughulikia mwenyewe na kwenda utakako; lakini utakakapokuwa mzee utainyosha mikono yako, na mwingine atakufunga na kukuchukua usikotaka" alisema hatimaye mtu huzeeka akaishiwa nguvu na kutegemea msaada kwa wenye nguvu na baada ya uzee mauti humkumba na kufunga historia yake duniani, ama akisubiri ufufuo ama vinginevyo. Wanahistoria wanasema Petro aliuwawa mwaka 68BK na kuangikwa msalabani kichwa chini na miguu juu. Yule aliyekuwa na urahisi wa kuropoka mambo bila kufikiri, na kuwa na haraka ya kujibu mambo bila kuongozwa na Yesu sasa alikuwa mtu wa karibu na moyo wa Yesu. Mtu aliyekuwa na hekima, na akaliongoza kanisa kwa njia mbalimbali, na kuleta wengi kwa Kristo. Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi Lake. Kuna mambo mengi sana tusingejua kama Petro asingeuliza, ambayo tungetamani tuyajue! Katika kuzikabidhi kwa uwakili wake roho alizozifia, Kristo alimpa Petro uthibitisho wenye nguvu zaidi kwamba alikuwa na ujasiri naye katika urejesho wake. Akisha kusema vile alimwambia Petro amfuate, ila Petro badala ya kushughulikia yake akaanza kuchunguza ya Yohana, ambaye aliandika kwenye kitabu chake kwamba yeye ndiye alipendwa zaidi na Yesu! Petro akauliza "BWANA na huyu Je?" Yesu akamwambia ikiwa nataka huyu aishi mpaka nitakapokuja mara ya pili, nijapo je, yanakuhusu nini wewe? Wewe njoo unifuate." Alitaka Petro aweke macho yake na matumaini Kwake na si kwa watu wengine. Hata leo tusiwe na viwivu kwa watoto wengine wa Mungu, kwamba wanabarikiwa kwa kuhubiri na watu wanabadilishwa, au wana mali kupita sisi, au wanaonekana maisha yao ni rahisi kuliko sisi. Mungu anatupenda, Naye anajua kipi kinamsaidia nani, na kwa namna gani.

Basi Neno lile likaenea kati ya mitume kwamba Yohana hatakufa, ila Yesu hakusema vile bali Alisema "ikiwa nataka huyu akae hata nijapo imekupasaje wewe?' Kila mtu ana jukumu tofauti alilopewa na Mungu. Mfano mzuri ni wa Yohana mbatizaji, alijua ameshafanya zamu yake, japo alisikia Yesu anakula na kwenda sherehe kwa watu, alijua kwamba sehemu yake imefikia kilele pale. Naye Yesu akawa na wanafunzi ikafika wakati wake wa mateso pia, akapita na kushinda. Mwishowe wakaja mitume, nao wamefanya zamu yao. Leo nasi ni zamu yetu, hivyo tusiwe na shauku kujua biashara za watu wengine, bali tujihangaishe kujua zetu. Jambo kubwa ni kumtazama Yesu, ili tubadilishwe tuwe kama Yeye kutoka utukufu hadi utukufu.
Petro hakupewa mamlaka ya kuangalia wengine, ila aliambiwa ya wengine hayakuhusu, wewe nifuate Mimi. Petro baadaye kwenye barua anasema 1 Petro 5:3,4 "Tusione ni jambo la ajabu kuangukia mateso….." Yohana aliandika na kushuhudia yale Yesu alisema kwa macho yake na masikio (ushahidi wa kuona, ushahidi wa macho, si wa kuambiwa). Yohana alimwona Yesu kabla ya kufa na baada ya kufufuka. Yohana alimwona YESU katika mwili Wake wa utukufu. Kuna mambo mengi aliyoyafanya Yesu ambayo yakiandikwa moja moja, nadhani

hata ulimwengu usingetosha kwa vile vitabu vilivyoandikwa. Hata kule mbinguni tutajifunza na kutofikia mwisho wa elimu ya Maneno ya Mungu.


Ni ufahamu mpana ambao tutaendelea kujifunza milele zote. Kisa cha wokovu chenyewe tu! ni cha ajabu mno. Tutafundishwa miaka mingi ya kutosha, na wala tusifikie kikomo cha kujifunza. Bado tena, kutakuwa na mengi ambayo inabidi kujifunza tena na tena.

*Kipengele kingine cha ombi linaloshinda, lenye ustahimilivu na lenye ushawishi ni imani. “Yeye amwendeaye MUNGU lazima aamini kwamba Yeye Yupo, na kwamba Yeye huwapa thawabu wale wamtafutao.” (Waebrania 11:6). Kristo anasema, “Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” Marko 11:24. Je! Tunamwendea na kumchukua kutokana na Neno Lake?
----------------------------

Maswali: Yesu alimwimarishaje Petro? Kwa nini watu wanamkana Yesu leo? Mimi nimeshawahi kumkana Yesu kwa jinsi mbalimbali, Je, wewe umemkanaje Yesu? Je, umeungama? Petro aliambiwa atakufa kifo gani? Kwa nini Petro aliona wivu kwa Yohana? Kwa nini ulimwengu hauwezi kutosha kuandika habari zote za Yesu? Twawezaje kumwimarisha rafiki aliyekosa leo?

**SIKU YA 290.**
**(Oktoba 16)**

# Yesu Anapaa juu mbinguni.



***Mathayo 28, Luka 24, Marko 16 na Matendo 1.***

Yesu alichagua mlima wa mizeituni kuwa mahali pa kupaa Kwake. Hapa Yesu alikuwa ameomba mara nyingi na mitume. Alikuwa amekaa nao kwa miaka 33 1/2. Alikuwa amepata nao shida, na matukano ya watu, hata na kuchekwa pia. Alikataliwa na mwishowe kuuwawa kwa kifo cha msalaba. Binadamu walimkataa bali bado alikuwa na upendo nao. Mitume walikuwa na udhaifu wao bali walimpenda Yesu, kwa upendo wa Kweli na wa dhati. Japo walikuwa si wakamilifu, Yeye aliwasafisha.

Yesu akaja kwao, akasema nao, akawambia "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Enendeni mkayafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu. Na kuwafundisha kuyashika yote Niliyowaamuru ninyi, na tazama Mimi nipo nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Aaminiye ataokoka asiyeamini atahukumiwa." Akawaambia ishara hizi zitafuatana na wao waaminio "Kwa Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya. Watashika nyoka hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa, wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya."

Aliwaambia pia "kama Baba alivyonituma, Mimi Nami nawatuma ninyi ulimwenguni kuwaambia habari njema", Naye akisha kusema hayo akawavuvia Roho Mtakatafu. Hivyo mitume walianza kupewa Roho Mtakatifu na Yesu akiwa nao. Waliombana misamaha, wakajifikiria walivyotaka ukubwa, wakaacha ya kale mabovu, na kuanza kufurahiana na kufanya kazi pamoja. Walakini mtume Tomaso aitwaye pacha hakuwa pale na wanafunzi wengine wakati alipokuja Yesu. Wanafunzi wengine walimsimulia wakisema "tumemwona BWANA", Naye akawaambia kwa kutoamini "mimi nisipoziona mikononi Mwake kovu za misumari, na kutia kidole

changu misumari ilipokuwapo, na kutia mkono wangu katika ubavu Wake sisadiki hata kidogo."

Ikawa baada ya siku nane, wanafunzi Wake walikuwamo ndani tena na Tomaso alikuwa pamoja nao safari hii. Yesu akaingia ndani tena milango ikiwa imefungwa akisema "amani iwe kwenu", kisha akamtazama Tomaso hapo hapo na kusema "Tomaso lete hapa kidole chako; uitazame mikono Yangu; ulete na mkono wako uutie ubavuni Mwangu, wala usiwe asiyeamini bali aaminiye."

Tomaso akashtuka, maana mtu wa kawaida hawezi kujua aliyosema au kuwaambia wanafunzi wenzake kabla. Tomaso alipatwa na unyenyekevu, hata bila ya kugusa kovu za Yesu Alisema "BWANA wangu na Mungu wangu!" Ndipo Yesu Akasema Maneno kwetu wote tunaosoma "Wewe Tomaso, kwa kuwa umeniona na kusadiki, wa heri wale wasioniona wakasadiki." Hao ndiyo sisi tunaoishi leo, pengine Yesu hawezi kututokea leo katika maisha yetu, bali tutamwona akija mara ya pili, ila tuna baraka zaidi au tu heri sisi ambao hatukumwona na tunamwamini au kumsadiki, tukimtegemea Yeye katika kila nyanja ya maisha yetu iwe ni mahitaji, elimu, magonjwa, furaha na mengine mengi.

Basi kuna ishara nyingi Yesu alifanya mbele ya wanafunzi Wake zisizoandikwa katika kitabu hiki cha Biblia, lakini haya yaliyoandikwa na tunayasoma leo, yameandikwa ili tupate kuamini kwamba Yesu Ndiye Kristo, Mwana wa Mungu, na KUAMINI vile tuwe na UZIMA WA MILELE. Walikusanyika watu zaidi ya 500, kwenye mlima wa mizeituni Galilaya, kule Bethania. Baada ya kusema Enendeni kote duniani mkawafanye mataifa kuwa wafuasi Wangu. Hii ilikuwa kama mara ya kumi na moja Mwokozi aliyefufuka alijionyesha kwa wanafunzi Wake.

Baada ya Yesu kusema na mitume, kawaongoza Bethania, ambayo ni chini ya mlima wa mizeituni, akainua mikono Yake akawabariki. Ikawa katika kuwabariki alijitenga nao, yaani akawa anapaa akichukuliwa juu mbinguni. Wakamwabudu na kusujudu akipaa juu mbinguni, wakimtazama akitokomea na mawingu yakamfunika. Jambo la furaha kuu, maneno ya kibinadamu yanashinda kueleza furaha yangu kwani, nasi ndiyo tutakavyopaa kwenda juu mbinguni Yesu atakapokuja mara ya pili. Safari hii ya kwenda mbinguni huku tukiona sayari zingine, itakuwa ya ajabu, tunapoelekea mbinguni. Tutaona mengi, yale wanasayansi wanasimulia kidogo sana (kinong'oningo), yale mabilioni ya sayari yanayochukua miaka mamilioni kufika kwa maroketi, tunaambiwa tutasafiri kwa muda mchache tu, pengine isipite wiki, tukiangalia yote ya ajabu.

Sayari za Mekuri, Jupita, Venusi na zingine nyingi maana elimu ya binadamu inatueleza punje moja ya mchanga ya elimu ya sayansi. Kutakuwa hakuna haja ya kufunga mkanda, wala kuwa na chombo. Tutakuwa tunatazamana na wengine nje kwa nje tukipaa na kuzungumza na kuangua vicheko vya furaha tukisimuliana jinsi mambo yalivyokuwa duniani. Shida zetu zitaonekana ndogo ukilinganisha na zawadi ya mazuri yale Mungu ametutayarishia. Tutavinjari na kuelezwa mengi na Kiongozi wetu. Safari hii ya mbinguni, si ya kukosa.

Nafikiri itachukua siku chache tu kufika, na si kama roketi ya kwenda mwezini, ambayo inaenda maili 17,000 kwa saa na kufika mwezini kwa siku tatu, ambao ni karibu sana na dunia. Kutoka na utalaamu mdogo na habari finyu tulizo nazo, ni kwamba kule mbinguni ni mbali zaidi ya mwezi ulipo! Pengine mabilioni ya maili toka kwetu duniani! Ila habari kamili tulizo nazo ni pazuri mno, maana macho hayajaona, wala masikio hayajasikia, wala hayajaingia katika mawazo ya mwanadamu yale ambayo Mungu ametutayarishia. Hebu turuke ruke kwa shangwe, na kupiga makofi! Unganisha mikono yako basi!

Hapo hapo wakatokea watu wawili wenye nguo nyeupe, huenda walikuwa Malaika wakasema "Enyi watu wa Galilaya mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakakuja jinsi hiyo hiyo mlivyomwona akienda Zake mbinguni. Hatarudi kwa siri, au kinyamela, na wala hatakanyaga chini ya ardhi bali tutanyakuliwa juu kumlaki mawinguni. Hili ni Fundisho muhimu mtu akikwambia ni Kristo. Je upo tayari kumlaki Yesu mawinguni?

Kisha wakarudi Yerusalemu kwa furaha kuu. Watu walitegemea marafiki za Yesu watasikitika baada ya kuachwa, wakastaajabu, sura zao ziking'aa kwa furaha, ambayo yatoka mbinguni. Wakawa tayari kushuhudia watu habari njema za ufufuo wa Yesu, na kurudi Kwake mbinguni, na wengi wakaamini kwa sababu hiyo. Mitume walijua mbinguni kuna rafiki yao Yupo kule, na kwamba anawajali sana. Wakachukua muda kusali na kuongea na Rafiki yao mpendwa, wakijua Rafiki Huyu atawapa lolote waulizalo kwa Jina Lake, ili furaha yao itimilike. Na Roho Mtakatifu Naye akawaletea furaha zaidi, kama Yesu alivyowaahidi. Yesu alifika kwa Baba Yake mbinguni na kuketi mkono wa kuume wa Mungu.

Mitume wakawa wanazungumza kuhusu BWANA wao, wakakumbushana mengi "unakumbuka alisema hivi" au "unakumbuka wakati alipokuwa anapaa alisema nini" Watu wakaja wakawauliza maswali mengi, wale ambao hawakujaliwa kuona kupaa Kwake. Nao walikuwa daima ndani ya hekalu, wakimsifu Mungu kwa furaha, sasa ilikuwa imeingia kichwani, wakarudi nyuma na kustaajabu yale waliyopitia! Wakakumbuka ahadi ya kumngoja Yerusalemu.

Wengi siku hizi wamechora picha za malaika kama vitoto vidogo, au wasichana warembo, ila kulingana na Maandiko, na wale waliotokewa na hao malaika, wanadai kuwa malaika ni watu wazima na wanaume. Huenda ikawa Malaika hawana jinsia ila yote hayo tutayajua siku moja. Malaika hawa waliwapa watu faraja ya kurudi kwa Yesu, kwamba hatarudi kwa siri ila kila jicho litamwona. Atakuja na Malaika Zake na kama Mfalme Mwenye enzi. Ameenda kutayarisha makao kwa ajili yetu, anakuja ili alipo nasi tuwepo.

Malaika walifurahi kumpokea BWANA wao mbinguni, alipofufuka katika wafu. Pengine wale wazee 24 waliandamana Naye kuwa mazao ya kwanza ya ufufuo. Tunasoma Zaburi 24:7-10, Malaika wakiimba wimbo wa kumkaribisha Yesu walijibishana pambio hilo "Inueni vichwa vyenu enyi malango, inukeni, enyi malango ya milele Mfalme wa utukufu apate kuingia. Ni nani Mfalme wa utukufu?

BWANA Mwenye nguvu hodari, BWANA hodari wa vita. Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Naami viinueni enyi mlango ya milele. Mfalme wa utukufu apate kuingia. Ni nani Huyu Mfalme wa utukufu? Bwana wa majeshi, YEYE Ndiye MFALME wa utukufu."

Kisha Malango yakafunguliwa ili Mfalme apite. Kulikuwa na sherehe kubwa mbinguni kumkaribisha Mwokozi nyumbani, na kusherehekea ushindi. Yesu alikuwa duniani miaka 33 na ½. Malaika wa mbinguni furaha yao kubwa ni kukaa karibu na Yesu. Wanamkimbilia na kutamani wakae karibu Naye saa yote! Hebu nasi tumwombe Mungu atusaidie tuwe na shauku hiyo ya kutulia kwa Yesu, tukibarizi na kumtazama uso Wake wa upendo.

Akifika tu, baada ya kupunga mikono, alimkaribia Baba Yake na kumwonyesha makovu Yake ya kichwani, ubavuni, mikononi na miguuni. Mungu na Mwana Wake walikuwa na kikao kabla hajaja duniani, na Mwana akawa rehani kwa ajili yetu binadamu. Yesu akatoa ombi zito la upendo wa pekee tena "Baba Nataka wale ulionipa, wawe Nami hapa." Wale "alionipa au aliompa" ni wewe na mimi. Mungu na Mwana Wake, wakawa pamoja tena, basi Malaika wote wakamwabudu. Mbingu ikajaa furaha tele, kwani Upendo umeshinda uovu. Sauti ikasikika ya Ufunuo 5:13 kutoka kila kiumbe "Baraka na heshima na utukufu na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na Yeye Mwana-Kondoo hata milele na milele. Amina."

Nimefikiri kuwa huu ulikuwa mwonekano wa ajabu kiasi fulani kwani Yesu alipotoka mbinguni alikuwa hana umbo, na sasa alirudi na umbo la mwanadamu. Tena alikuwa ameishi na binadamu wenye utashi wa chini, Naye alikuwa anarudi kuishi na BABA Mwenye Maarifa yote, uwezo wote, na anayeweza kuwepo mahali popote. Mfano wa kutoa picha hafifu utakuwa, ni kama uliishi na mtoto wa mwaka mmoja, miaka 33 na 1/2 na sasa unaenda kuishi na Profesa mzee anayefundisha chuo kikuu. Neno alikuwa amefanyika binadamu na kurudi mbinguni. Mungu BABA akawa akizungumza na Mwana Wake ambaye sasa alikuwa na mwili wa binadamu. Yule ambaye milele zote aliweza kuwa popote, sasa alikuwa mahali pamoja. Alimsikia Mwana-Wake akimsimulia kuhusu marafiki Zake duniani. Ni kama wewe utokapo shule ukamsimulia baba yako kuhusu marafiki zako unaowapenda. Kweli mbingu ilikuwa imeunganishwa kwa gundi kubwa kupita zote kupitia Yesu.

Mbingu na dunia zimeunganishwa milele, na Yesu, BWANA wetu na Masihi wetu. Yesu amefufuka na kupaa na anaishi milele. Hivyo ana uwezo wa kutuokoa wote tunaomjia Mungu kupitia Kwake, kwa kuwa anaishi, kutuombea na anao ukuhani usioondoka Waebrania 7:25. Yesu si mtu mwema tu aliyekufa kwa ajili ya dhambi zetu, bali ni Mungu aliyefufuka na kukaa upande wa kuume wa BABA. Akiishi kwa ajili yetu atuombee.

*Tunapokuja kuomba rehema na baraka kutoka kwa MUNGU tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha mioyoni mwetu. Je! Tunawezaje kuomba, "Utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu," na bado tunaendekeza roho ya kutosamehe? Mathayo 6:12. Ikiwa tunatarajia maombi yetu wenyewe yasikilizwe lazima tusamehe wengine kwa njia ile ile na kwa kiwango kile kile tunachotarajia

kusamehewa.

----------------------------

Maswali: Walikuwa takribani ya watu wangapi waliokuwa na Yesu mlima wa mizeituni? Aliwaambia wafanye nini? Yesu aliahidi nini kwa wanafunzi Wake? Ahadi hii ingesaidia nini? Kupaa ina maana gani? Nini kilitokea wakati wa kupaa? Tomaso alikuwa na shida gani? Watu wawili wenye nguo nyeupe walisemaje? Twawezaje kuondoa mashaka ya 'Tomaso'? Kutokana na sura hii, elezea jinsi kuja kwa Yesu kutakavyokuwa? Je, upo tayari leo kumlaki Yesu mawinguni? Je, ile miaka 30 ambayo Yesu alikaa nyumbani kabla ya huduma ilisaidiaje kazi Yake?

**SIKU YA 291.**
**(Oktoba 17)**

# Je, Yesu anafanya nini mbinguni sasa? "Tuna Rafiki mbinguni."



Yesu aliishi miaka thelathini na tatu na nusu duniani, kama binadamu na Mungu. Watoto wengi wana shauku kujua Yesu alipoenda mbinguni mambo yalikuwaje huko, na anafanya nini huko sasa? Maandiko yanatupa fununu ya mambo ambayo Yesu anayafanya kwa sasa. Kwa mujibu wa kitabu cha Zaburi, Yesu alikaribishwa na malaika alipoingia mbinguni. Malaika, wazee, na viumbe wale wanne, wanamwabudu mbinguni. Yesu Mwana-Kondoo aliyechinjwa, Amestahili kuupokea uweza, mamlaka, utajiri, hekima, nguvu, heshima, utukufu na baraka. Mbinguni lilisikika pambio, viumbe vyote vikiimba "baraka na heshima, utukufu, na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, Milele na Milele."

Wakati mitume wanapokea Roho Mtakatifu chini hapa duniani, Yesu alisimikwa kwenye Mamlaka ya Kuhani, na mfalme wa mbiguni. Hatujui kama BABA Yake alisaliminaje Naye baada ya kumaliza kazi hii ngumu. Wote wawili walikuwa wamejitoa mhanga. Alikuwa amekaa na marafiki Zake miaka 33 ½ akizungumza na BABAYE kwa kusali na sasa amerudi nyumbani tena mbinguni na kukabiliana

uso kwa uso na Babaye. Mambo yahusianayo na Uungu hatuyajui sana, tutayazungumza machache kama Biblia inavyosema. Twapasa kuepuka kabisa kuandika yale yasiyonenwa mle! Kitabu cha Waebrania kinatuambia vyema kuhusu kazi ya Yesu kule mbinguni alipopaa kuliko kitabu kingine chochote. “Yeye ni mng’ao wa utukufu Wake na chapa ya nafsi Yake. Akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa ukuu huko juu, amefanywa bora kupita malaika, kwa kadiri ya Jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko lao.” YEYE Ndiye anatupa pumziko la moyo, anatuweka huru- Waebrania 4:9. Kuna haja ya kusoma zaidi kwenye Biblia kuhusu Masihi maana tunaambiwa “Ndani Yake Yeye hazina zote za hekima na maarifa vimesitirika”. Hakika sote tunahitaji hazina hizi ambazo zimesitirika ndani Yake. Yeye Ndiye Kweli, Njia na Uzima. Yabidi tukae ndani Yake na kujisalimisha Kwake. Stefano katika matendo saba alimwona Yesu katika maono akiwa mkono wa kuume wa BABA Mungu. Zaburi 110: 1 pia yasema hivyo pia. Makuhani wa kibinadamu walisimama wakitoa dhabihu zile nyingi za wanyama ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi. Ila Yesu “Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu” amekufa mara moja tu atuondolee dhambi milele zote, maana ametoa dhabihu moja idumuyo hata milele.

Yesu amemaliza kazi ya kutoa kafara kwa wokovu wetu na sasa Yupo mbinguni kama kuhani, akitunufaisha wafuasi Wake. Yesu ni bora kuliko Musa, Yoshua, Haruni au Malaika hivyo ana ukuhani bora na Agano bora kwetu. Yeye ana ukuhani wa milele, maana binadamu waliokuwa makuhani walikufa ila Yeye anakaa milele kwa sababu hii aweza kutuokoa kabisa wote sisi tumjiao kwa maana Yeye Yu hai siku zote ili atuombee. Si kwamba Yesu ametoa dhabihu bora kupita zote kwetu ili tuokolewe tu, bali pia ni Kuhani bora, anayetuombea na kutupatanisha na Mungu kuliko kuhani yeyote yule. ANA UWEZO hivyo hatuna haja ya kuwa na hofu. Mkono Wake haujapunguka usiweze kuokoa. NI MWEZA, ndiyo maana anaitwa MWENYEZI MUNGU. Yohana aliwaonyesha na kuwaambia watoto “watoto wadogo msitende dhambi, Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki. Ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu, na dhambi za uliwemwengu mzima.” Yohana anasema wazi kwamba sisi binadamu tunatenda maovu, ila tuungame dhambi zetu bila kuficha au kupiga chenga, kwa kutoa udhuru kwamba tuna ulemavu fulani wa maumbile, au ni kutokana na hali za wazazi wetu. Tuna mtetezi wetu Yesu, hivyo tuje Kwake kwa ujasiri mkubwa kwenye kiti Chake cha enzi, ili kupata msamaha na rehema.

Paulo anasema “Je, Mungu akiwa upande wetu ni nani aliye juu yetu, Yeye asiyemwachilia Mwana Wake Mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sote aweza kukosa kutukirimia na mambo yote pamoja Naye?” Je ni nani aweza kututenga na upendo wa Kristo? Jibu, Je, ni shida, dhiki, adha, njaa, kukosa nguo, umasikini, hatari, upanga au hata mauti. La! hivi haviwezi kututenganisha na upendo wa Kristo Yesu. Tuna rafiki mbinguni, leo, Naye ni Yesu Kristo. Yesu alisema BABA hamhukumu mtu yoyote ila amempa Mwana au Yesu hukumu. Hivyo Yesu Ndiye Jaji na mtetezi wetu. Unapoendelea kuwa na imani na mahusiano na Mungu kupitia kwa Yesu; kamwe huna haja ya kuogopa. Kwa nini hauna haja ya kuogopa hukumu? Kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yetu, na alifufuka, na sasa yupo mkono wa kuume wa Mungu BABA akiombea wale wote wanaomwamini, kama Kuhani wao mkuu. Hakuna

hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, amechukua adhabu yetu.

Ni vyema kujua kuna hukumu kabla ya kwenda mbinguni, ila Kuhani wetu ndiyo hakimu na pia mtetezi wetu. Hakimu Yuko upande wetu, hivyo tu salama Ndani ya Yesu. Na huu ndiyo ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake atusikia. Tuna Rafiki mbinguni, anayejibu maombi yetu, Ambaye alifanyika kama binadamu afanane nasi, hivyo ajua uzoefu wetu na anapenda kujibu maombi ya wale wanaomtumaini na kumtegemea. Hujibu maombi ya watoto Wake wadogo na wakubwa. Huduma ya Yesu ya maombi ndiyo kiini cha huduma Yake kama Kuhani leo. Hebu tuwe na ujasiri, mambo mengi yatufika kama binadamu iwe ni maumivu, umasikini, maadui, shida na kutetereka; ila tujue japo kuna changamoto duniani, tuwe na ujasiri kwamba tuna Rafiki mbinguni Aliye tayari kujibu maombi yetu.

Kazi nyingine Yesu anafanya mbinguni ni hukumu. Wayahudi walikuwa na siku ya upatanisho (Yom Kippur), hii ilikuwa siku ya hukumu. Biblia yatuambia katika Danieli 7 "Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja Aliye Mzee wa siku ameketi, mavazi Yake yalikuwa meupe kama theluji na nywele za kichwa Chake kama sufu safi, kiti Chake cha enzi kilikua na miali ya moto, na gurudumu Zake moto uwakao. Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele Zake; maelfu elfu wakamtumikia na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele Zake hukumuni wakisimama mbele Zake, hukumu ikawekwa na vitabu vikafunuliwa."

Kwa lugha ya kibinadamu, Yesu atakapomaliza hukumu, ataweka kando mavazi Yake ya ukuhani, na kuvaa mavazi ya Mfalme Mshindi. Lugha ya kibinadamu inashindwa kuelezea jinsi ambavyo mamilioni ya Malaika na kiti cha enzi kinavyoonekana. Hukumu kuwekwa, yaonyesha wazi kwani vitabu vilifunguliwa. Mungu anataka dunia na sayari zingine zote zenye viumbe vijue kwamba amefanya kila alichoweza kushughulikia tatizo la dhambi. Tatizo la dhambi, ndilo lilifanya Yesu aje na kuzaliwa kama binadamu, yaani Emanueli, yaani, Mungu pamoja nasi, akaishi, pamoja nasi. Viti vya enzi kuwekwa na vitabu kufunguliwa yamaanisha hukumu imefikia wakati Wake, au mwisho wa mambo ya historia ya dunia.

Kitabu cha Danieli saba kimezungumzia hukumu wazi wazi na kusema kwamba Yesu au Mwana wa Adamu Ndiye ameshinda katika hukumu na "ufalme na mamlaka na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote watapewa watu watakatifu wake Aliye juu, ufalme Wake ni ufalme wa milele na wote wenye mamlaka watamtumika na kumtii." Huo ndiyo ukawa mwsho wa jambo lile. Mungu hapokei rushwa au hapendelei mtu mbaya kwa vile ni rafiki Yake. La! Basi tumche Mungu na kumtukuza maana saa Yake ya hukumu imewadia.

Yesu ni Mwokozi wetu, na Hakimu pia. Wote waliokubali kazi Yake ya wokovu, hawana haja ya kuhofu kuhusu hukumu ya mwisho. Biblia inasema hukumu ni habari njema kwao, yaani injili. Wale watakatifu wanaoteseka wanataka hukumu na wanamwuliza Mungu 'Ee Mola Mtakatifu Mwenye Kweli, hata lini utaleta hukumu ili haki yetu isipotee?" Watakatifu wanafurahia hukumu maana wanajua Mungu ni wa haki kuliko binadamu. Ni bora kuangukia kwenye mikono ya Mungu

kuliko binadamu mara zote. Madhumuni ya hukumu si kufanya watu wasipate ufalme, bali kuwafanya wengi inavyowezekana waende na Yesu nyumbani mbinguni atakapokuja tena, na kuishi Naye milele zote kwenye ufalme Wake.

Kwenye hukumu yataletwa maisha yetu na mioyo yetu, kila mtu atalipwa kwa kadiri ya matendo Yake, na ndiyo maana Yesu alisema "Si kila mtu aniitaye BWANA BWANA ataingia ufalme wa mbinguni bali Yeye afanyaye mapenzi ya BABA Yangu." Kisha mlango wa rehema utafungwa siku moja na "Mwenye kudhulumu atazidi kudhulumu na mwenye uchafu atazidi kuwa mchafu, bali mwenye haki, atazidi kufanya haki na Mtakatifu atazidi kutakaswa." Yesu atakuja na ujira Wake upesi, kumlipa kila mtu kwa kazi yake ilivyo. Tuwe na ujasiri na kukaribia Kwake kwa imani tukijua, hukumu i upande wetu. Kufungwa mlango wa rehema kutatokea muda mfupi kabla ya Yesu kuonekana mawinguni. Hapa ndiyo watakatifu watanyakuliwa na Yesu atakayekuja na Malaika na parapanda.

Wakati huu kutakuwa na shida kwani mlango wa rehema ukifungwa Shetani atakuwa na mamlaka ya kufanya anavyotaka popote. Ndipo mambo mengi yatakuwa holela na ya ajabu. Uchumi, matukio ya hatari na kutisha na mengineyo yatatokea. Ila tujipe Moyo, Yesu alisema "Tusifadhaike mioyoni mwetu, tumwamini Yeye na BABA wa mbinguni." Yesu ni Mwanzo na Mwisho, Alfa na Omega yaani ukamilifu na umilele wote, twaweza kumtumaini Yeye bila shida yoyote.
Tuna wakili, na mtetezi, ambaye ana uwezo, Hivyo tuje kwa ujasiri Kwake, kwenye kiti cha enzi kwa maombi, nasi tutasamehewa na kutakaswa.

*Lazima tuishi Maombi yetu ikiwa yataenda kujibiwa — Tunapaswa kuomba na kukesha katika maombi, ili kusiwe na mapishano katika maisha yetu. Hatupaswi kukosa kuwaonyesha wengine kwamba tunaelewa kuwa kukesha katika maombi kunamaanisha kuishi maombi yetu mbele za MUNGU, ili kwamba Yeye ayajibu.
----------------------------

Maswali: Yesu aliishi miaka mingapi duniani? Taja kazi za Yesu leo mbinguni? Kwa nini hatuna haja ya kuogopa hukumu? Kwa nini tuwe na ujasiri? Unafanya jambo gani kujitayarisha na hukumu leo? Kwa nini twapasa kumcha Mungu na kumtukuza?

**SIKU YA 292.**
**(Oktoba 18)**

# Kusimulia Kisa cha Wokovu kwa dakika tatu!- Wokovu ni nini?



Kwa sababu sasa tumemaliza vitabu vya injili, yaani habari njema kwa sisi sote Wana wa Adamu. Je, waweza kusimulia kisa cha wokovu kwa dakika chache kwa yule asiyemjua Mwenyezi Mungu au Yesu kabisa? Ni muhimu uweze kufanya vile. Kwa kufufuka kwa Yesu tumepata ondoleo la dhambi, kuna furaha mbinguni maana watu wanaokolewa sasa kupitia kifo Chake. Kwamba sasa binadamu hatuwezi kupotea milele ni Mwujiza wa kusimulia milele zote. Watu walianza kuonja tunu hii toka msalabani siku ile, yaani yule mwizi aliyesulubishwa na Yesu, na hata Akida.

Kwa kuwa wewe sasa ni mwanafunzi wa Yesu, na si mfuasi tu, yapasa uende kuwasimulia wengine. Wewe sasa ni mtume wa Yesu. Mwombe akupe Roho Wake ili uweze kuishi maisha ya utauwa na kisha uwashuhudie wengine. Mwanafunzi au mwongofu anajifunza, bali mtume anatumwa kumshuhudia Mungu kwa wengine. Ukutanapo na watu waambie matendo makuu ya Mungu, ndiyo jinsi ya kumshinda Shetani "wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo na kwa Neno la ushuhuda wao" Ufunuo 12:11.

Rafiki, Je, unajua njia cha wokovu? Je, unajua kwamba Mungu yupo na ana mipango kwa kila mtu ikiwa ni pamoja na wewe? Je, unajua jinsi ya kuwa na amani na Mungu ndani ya moyo wako? Inawezekana kabisa kuwa na amani katika mahangaiko na mifadhaiko ya maisha haya. Majibu kwa maswali yako yote yapatikana kwenye Neno la Mungu. Je, wajua nini kinatokewa ukifa? Je, Yawezekana kuishi maisha ya furaha, amani na kuridhika moyoni? Ndiyo yawezekana kabisa na siri yake iko kwenye Neno la Mungu, na haihusiani na kuwa tajiri, au mwenye akili nyingi, mtu mwenye talanta nyingi!

Neno la Mungu katika Warumi 3:23 linasema "wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Linaendelea kusema "hakuna mwenye haki, hata mmoja, wote wamepotoka, wameoza wote pia, Hakuna mtenda mwema, La! hata mmoja" Warumi 3:10-12. "Mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele" Warumi 6:23. Tukisema hatuna dhambi twajidanganya wala Kweli haimo ndani yetu. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni Mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote 1 Yohana 1:8,9. Basi ili kupata wokovu twapasa kuziungama dhambi zetu na toba ya dhati "Tubuni basi mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako Kwake BWANA" Matendo 3:19.

Lazima tukiri kwa midomo yetu kwamba Yesu ni BWANA na Mwokozi wetu. "Ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni BWANA, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka." Waweza kuishi maisha ya furaha na yenye kuwa na maana na manufaa. Ndiyo! waweza kumjua Mungu binafsi; na majibu yote yatoka kwenye Neno la Mungu. Kwa vile umeshajua haya yote, sasa nenda kawaambie wengine mambo makuu ambayo Mungu amekufanyia na kisa cha wokovu na cha thamani. Waambie mpango Mungu baada ya maanguko ya wazazi wetu bustani ya Edeni. Mpango wa kumtuma Mwana Wake "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila amwaminiaye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Weka jina lako pale "ili kila" ilipo.

Mungu alimtuma Mwanawe "ili Neema akimwamini asipotee bali awe na uzima wa milele." Yesu alitendewa sisi tunavyopaswa kutendewa, ili tuweze kutendewa Yeye anavyostahili kutendewa. Alihukumiwa kwa dhambi zetu, ambazo hakuzifanya, ili kusudi tuokolewe na haki na wema Wake, ambao sisi hatukustahili. Alikufa kifo chetu, ili tupate uzima wa milele, tunaponywa kwa sababu ya majeraha Wake.

Endelea kukua kwa imani na kushika Amri Zake "Katika hili twajua ya kuwa tumemjua Yeye, ikiwa tunashika Amri Zake." 1 Yohana 2:3. Basi tutembee nuruni na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho na maji, kwa kubatizwa na kupokea Roho wa Mungu ili atuongoze katika yote. Kwa kuwa binadamu, alitufikia sisi binadamu, kwa Uungu Wake alishikilia enzi ya Mungu. Kama Mwana Adamu ametupa mfano, wa kuishi tukifuata Sheria za Mungu. Kama Mwana wa Mungu ametupa uwezo kwa kupitia uwezo Wake, Sheria za Mungu zaweza kutiiwa.

Kama umechukua hatua hizi, BWANA akubariki, umekuwa mtoto wa Mungu

aliyezaliwa upya. Yeye aliyeanza kazi njema moyoni mwako ataikamilisha, amesema alionipa BABA sitawapoteza kamwe, Amina. Yeye aweza kukulinda usijikwae na kukusimamisha mbele ya utukufu Wake bila mawaa katika furaha kuu, Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu Yesu Kristo, BWANA wetu; utukufu una Yeye, ukuu na uwezo, na nguvu milele zote. Amini Maneno Yake, omba aondoe kutoamini kwako. Ukisikia na kufuata haya, umekuwa tayari sasa hivi kumlaki Yesu mawinguni ajapo. Mtu akikuuliza Je, Yesu akija leo, utakuwa mbinguni? Sema Ndiyo! Mtu akikuuliza Je, umeokoka? Sema ndiyo! Endelea kusoma Neno Lake, na kuishi mtindo wa maisha Yake, Fuata Nyayo Zake Masihi kwa maneno mengine, hakika mbingu ipo karibu nawe ukifuata hatua hizi. Na unapotenda dhambi, ungama, na kisha ufuate tena njia sahihi ambayo Maandiko yanatuhimiza.

Ukisimulia kisa cha wokovu, wengine wameuliza utatu mtakatifu ni nini? Japo Neno hili halijaandikwa kwenye Maandiko, Mungu BABA, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu zaitwa nafsi tatu za Mungu mmoja au Utatu Mtakatifu. Hatuna Miungu watatu bali MUNGU mmoja na wa Kweli. Mfano huu ni kama kusema familia, ni baba, mama na mtoto. Familia si mtoto mwenyewe, au baba mwenyewe. Hakuna mwenye kujua sana siri hii ya Uungu, au kufanyika mwili, au kifo au ndoa takatifu, Biblia imeviita vitu hivi siri au mafumbo! Yale machache tunayoyajua ni yetu na watoto wetu na tusiyoyajua Mungu anayajua, nasi tunaendelea kumwomba Mungu atujulishe kutokana na mapenzi Yake, ila kikubwa ni kusonga mbele, kukaza mwendo kuelekea juu mbinguni, na kutokata tamaa! Tuombeane!
Endelea kusoma Neno Lake na kutenda vile linavyosema ukidumu katika sala. Maranatha (BWANA anakuja tena! karibuni).
Sasa itikia wito wa Mungu na kusema "Nitakwenda"

Mpendwa Yesu, "Mimi Hapa!" umeniita, na sasa nimeitikia. Mimi hapa Nitume. Sina mengi ya kuleta, lakini kufahamu kwamba upo upande wangu ni yote ninayohitaji kufahamu, kwani kwa wale unaowatuma, utawawezesha pia kufanya kazi zako. Hivyo, mimi hapa, Bwana. Mchukue mwanamume/mwanamke/mtoto huyu na ujitukuze Mwenyewe kupitia katika maisha yangu. Amina. "Nitume Mimi" Mungu, tunatambua kwamba kusudi la maisha yetu ni kudhihirisha tabia yako ya upendo kwa dunia hii. Tafadhali tutume katika shamba lako. Tuonyeshe mahali unapofanya kazi ili tuweze kuungana na Roho yako. Ongoza mawazo na mipango yetu Bwana, urafiki wetu, na jitihada zetu za utume. Tunataka kung'aa kwa ajili yako, Yesu. Tutume! Nitume! Nitakwenda! Amina.

*Maombi yetu Sio Amri za kumwamrisha MUNGU— Tunajua kwamba Yeye hutusikia ikiwa tunaomba kulingana na mapenzi Yake. Maombi yetu hayapaswi kuchukua mfumo wa amri, bali mfumbo wa maombezi Kwake Yeye ili afanye mambo tunayotamani kutoka Kwake.

--------------------------

Maswali: Msimulie mtu kisa cha wokovu kwa dakika tatu. Twajuaje kwamba tunakua kiimani? Maranatha maana yake nini? Nitajuaje kwamba nitaenda mbinguni? Yesu anakuja lini? Twawezaje kuishi maisha ya furaha, amani na kuridhika? Wawezaje kumweleza mtu Utatu Mtakatifu maana yake ni nini?

**SIKU YA 293.**
**(Oktoba 19)**

# Kungoja Roho Mtakatifu/Pentekoste Yerusalemu.

**Luka 24, Matendo 1 na 2.**



Yesu aliwaambia wanafunzi wakae Yerusalemu, na akawapa ahadi ya Baba Yake, kwamba watavikwa uwezo utokao juu, uwezo wa Roho Mtakatifu. Tumeona Yesu alipowaongoza Bethania, akainua mikono Yake juu akawabariki, na ikawa katika kuwabariki akajitenga nao, na akachukuliwa juu mbinguni, wakamwabudu; kisha wakarudi Yerusalemu wenye furaha kuu. Nao walikuwa daima ndani ya hekalu wakimsifu Mungu. Hawakujua kwamba uwezo watakaoupokea ni upi. Wakaulizana wakiwa katika maombi. Walikuwa na unyenyekevu wakipendana, na walipata ujasiri kwani hata watu waliwakejeli, ila walikuwa imara.

Jinsi walivyokuwa karibu na kila mmoja wao ndiyo walivyokuwa karibu na Mungu. Wakasameheana maneno makali na malumbano ya chuki waliyojibizana, wakaombana misamaha. Kila mtu akawa mcheshi na wa msaada kwa mwingine, hakuna aliyekuwa na hitaji ambalo mwingine angeweza kutatua akanyamaza kimya. Luka tabibu mpendwa ndiye ametuandikia kitabu cha Matendo, kama mwendelezo wa vitabu vya injili. Matendo haya ni Matendo ya Roho Mtakatifu

yakiwawezesha mitume kutenda mambo makuu walipokuwa wamkimhubiri Yesu. Matendo haya yanaendelea hata leo, yaani matendo yako, na yangu tukiongozwa na Roho wa Mungu.

Tabibu Luka hakuwa mmoja wa wale wanafunzi wa Yesu, bali alikuwa mwanafunzi kama wewe na mimi au muumini yoyote ampendaye Mwenyezi Mungu. Mfuasi huyu alikuwa Myunani au Mgiriki, siku zile aliitwa wa mataifa, yaani hakutoka Uyahudi kama mimi na wewe. Leo tunaitwa Wayahudi wa kiroho, na wale wa Israeli wanaitwa Wayahudi wa kimwili. Luka aliandika vitabu vyake vyote kwa Theofilo, ambaye alikuwa ana nafasi ya utawala. Maandishi Yake yanajulikana kuwa na uthabiti au uhakika kuliko maandishi yote ya kale (most authentic ancient literature). Kwani walienda kuangalia vitabu vya historia vilivyoandikwa wakati ule, miaka ya matukio, miji, majina ya watu, na wakakuta ni sahihi mpaka nukta! Mfano Kaisari Tiberia alipoanza kutawala, Kisiwa cha Malta n.k Daktari mmishenari huyu alifuatana na Paulo mtume aliyeitwa Sauli awali kwa safari za kupeleka injili kwa mataifa yote yaliyojulikana siku zile, Rumi ikitawala dunia. Alikwenda na Paulo hata Rumi, safari yake ya mwisho.

Siku Yesu alipochukuliwa na kupaa juu kwa Babaye ili aketi mkono Wake wa kuume, alikuwa amekwisha kuwaagiza kwamba Roho Mtakatifu atawashukia, wale aliowadhihirishia nafsi Yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa Kwake, ya kwamba Yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyohusu ufalme wa Mungu. Yesu alisema Yohana alibatiza ubatizo wa maji na toba bali wanafunzi Wake aliwaambia watabatizwa na Roho Mtakatifu baada ya siku si chache. Akawaagiza wasitoke Yerusalemu bali wangoje ahadi ya Baba wa mbinguni ili wapokee nguvu na kuwa mashahidi kuanzia kwa majirani zao Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, na mwisho wa dunia.

Walipokutanika pamoja walimwuliza Je BWANA wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme? Akawaambia si kwao kujua muda na majira aliyoweka Mwenyezi Mungu katika mamlaka Yake Mwenyewe. Nafikiri watu wangejua ni siku gani BWANA anakuja wangejitayarisha kwa ajili ya kuwa mbinguni, kwa woga (feki) ila mioyo yao haingekuwa na upendo wa Kweli kwa Mungu au kwa watu. Wangekuwa watu wa kuleta matatizo na shida mbinguni!

Baada ya watu wawili wenye nguo nyeupe (walikuwa malaika) kuwaambia zaidi ya watu 500 wa Galilaya kuwa Yesu atarudi kama alivyoenda kwa kumwona na wala si kwa siri (1Wakorintho 15:6), Walitoka mlima wa mizeituni, na kwenda Yerusalemu na walipoingia mjini Yerusalemu, walipanda gorofani walipokuwa wakikaa. Hapa Petro, Yohana, Yakobo, Andrea, Filipo, Tomaso, Bartholomayo, Mathayo, Luka, Simoni, na Yuda wa Yakobo na wanafunzi wengine wa Yesu zaidi ya mia, walikuwa wakidumu kwa maombi kwa moyo mmoja katika kusali, pamoja nao wanawake kama Mariamu mama Yake Yesu na ndugu Zake.

Petro alisimama gorofani kati ya hao watu 120 na kurudia unabii wa Yuda msaliti kwenye Zaburi. Unabii wataja hata kurudisha vipande 30 vya fedha kwa makuhani walionunua kiwanja cha kuzikia wageni, kiwanja hiki kikajulikana kama Konde

la damu au Alkadama. Kisha Yuda alijitia kitanzi akajinyonga, akiwa katika mti alianguka na mwili ukapasuka na utumbo ukatoka nje. Unabii wa Zaburi wasema “kikao chake na kiwe ukiwa wala asiwepo mtu mwenye kukaa humo; tena usimamizi wake autwae mwingine.” Akawaambia wanafunzi imefika wakati wa kuchagua mtu kushika nafasi yake ili namba yao iwe ile ile 12.

Basi walichukua watu wawili nao ni Yusufu aitwaye Barsaba au Yusto, kisha Mathiya na kuwapigia kura. Wakaomba uongozi wa Mungu “Wewe BWANA ujuaye mioyo ya watu wote, tuonyeshe ni nani uliyemchangua katika hawa wawili ashike kura ya utume ambao ameukosa Yuda kwa uchaguzi wake.” Kura ikamwangukia Mathiya naye akawa miongoni mwa wale thenashara (12). Yawezekana katika uchaguzi walipenda wapate mtu yule aliyemwona Yesu kwa macho, na akasikia Mafundisho Yake na akawa tayari kuwa mwanafunzi Wake. Mengi hayaelezwi kuhusu Mathiya kwenye Maandiko, ila hata Andrea na mitume wengine waliendelea na utume, bila mambo yao kuandikwa sana.

Basi mitume wakatoka wakihubiri kote kote, BWANA akitenda kazi nao, wakilithibithisha lile Neno kwa ishara zilizofuatana nao.

*Wakati wale wanaojua Ukweli wanapofanya mazoezi ya kujinyima yaliyoamriwa katika Neno la MUNGU, ujumbe utaenda kwa nguvu. Bwana atasikia maombi yetu ya kuongoa roho. Watu wa MUNGU wataruhusu nuru yao iangaze, na wasioamini, wakiona matendo yao mema, watamtukuza Baba yetu wa mbinguni.
--------------------------

Maswali : Kwa nini mitume walipiga kura? Je, Watu wenye nguo nyeupe waliwaambiaje watu? Luka aliwezaje kuandika kitabu cha Matendo? Je, matendo ya mitume yanaendeleaje leo? J,e kuna tofauti gani kupigiwa kura na kuwekewa mkono katika kutenda kazi ya BWANA? Taja majina ya mitume 12 baada ya Yesu kupaa kwenda mbinguni.

**SIKU YA 294.**
**(Oktoba 20)**

# Pentekoste.

**Matendo 1.**



Kabla ya kutoka kuhubiri, mitume walikaa pamoja siku kumi, wakijinyenyekeza, wakiombana misamaha wao kwa wao na kumwomba Mungu msamaha kwa kutoamini kwao maneno ya Maandiko na unabii. Neno Pentekoste lina maana siku 50 baada ya pasaka au baada ya Yesu kufufuka. Wanafunzi walipokea Roho Mtakatifu, Ambaye Mwenyezi Mungu aliahidi. Yesu aliwatokea kwa siku 40 baada ya kufufuka, na kisha akapaa kwenda mbinguni, nao wakampokea Roho Mtakatifu siku kumi baada ya Yesu kupaa.

Hata ilipotimia siku ya Pentekoste wale wanafunzi wa Yesu na mitume 12, wakiwamo mama ya Yesu na ndugu Zake na waumini wengine, wakiwa kwenye gorofa, mahali pamoja; kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawa na mtikiso, Mshindo au mngurumo huo ulisikika kwa watu waliokuwa nje. Kukatokezea ndimi za moto zilizogawanyika kwa kila mmoja. Kila aliyemtazama mwenzake alishangaa kuona ndimi hii juu ya kichwa chake. Ikaonekana kama nyumba ina mioto. Walikuwa na ukimya katika maombi ila mambo yalibadilika. Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha zingine kama Roho alivyowajalia kutamka. Mitume walitoka nje wasitake kukaa ndani tena! wakaanza kusimulia kisa cha Yesu, msalaba

na wokovu kwa furaha.

Kumwagiwa kwa Roho Mtakatifu kulitokea wakati waumini wa kila pande walikuja kutembelea Yerusalemu kwa ajili ya Pentekoste hivyo wengi walipata nafasi ya kusikia tukio hili. Walikuwa Wayahudi, watauwa na wa kila taifa chini ya jua. Wengine waliposikia tu ile sauti ya mvumo wa upepo walikutanika na kushikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia hawa wainjilisti 120 wakihubiri Injili kwa lugha tofauti zao, ambazo waliweza kuzitambua. Hawakuzungumza lugha au maneno yasiyo na maana bali lugha kamili za mataifa mbali mbali. Wakishangaa na kustaajabu waliambiana maana walijua mitume wote walitoka Galilaya. Ni Yuda msalitu tu, ndiye alitoka nje ya Galiya.

Wakajiuliza "Hivi hawa watu si ni Wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo na tupo mbali na kwetu? Warparthi, Wamedi, waelami, Wamesopotamia, Wayahudi, Wakapadokia, Waponto, Waasia, Wafiria, Wapamfilia, Wamsiri, Warumi, Wakrete, Waarabu na Walibia wa kule Kirene. Wote hawa walisikia kwa lugha zao; wakisema kwa lugha zao Matendo makuu ya Mungu. Wakashangaa na kuingiwa na mashaka, wakiambiana, "mambo haya yana maana gani?", kwani lugha za mashariki, magharibi, kusini, na kaskazini mwa nchi yao zilisikika. Roho Mtakatifu alitoa karama ya kunena kwa lugha kusaidia injili kwenda mbele, au kueneza Neno la Mungu. Nimekutana na watu walioenda nchi zingine kwa umishenari na walipozungumza watu waliwasikia kwa lugha zao katika nchi hizo, kama wale watu wa Maori kule New Zealand.

Siku hizi watu wanaenda shule kwa miaka mingi kujifunza kuzungumza lugha fulani, mfano kichina, kina alfabeti au tarakimu zaidi ya laki moja, ila mia mbili hivi ndiyo hutumika kwa mtu wa kawaida, kulinganisha na 24 za kiswahili. Watu wanachukua muda mwingi ili wapate kazi za biashara viwandani China. Mitume hawakuhitaji hayo yote. Kama kawaida ya binadamu, wengine wakaanza kejeli na dhihaka wakisema "wamelewa kupindukia na mvinyo mpya." Kejeli za namna hii ni njia ya kupunguza tusifikiri na kuamua kwa ajili ya Kumchagua Mwenyezi Mungu. Iwe mwiko kwetu kuleta mizaha kwenye mambo yahusianayo na Mungu. Kuchanganya Watu wengine huuita mwenendo huu ni "kukimbiza sungura au kupotosha malengo."

Watoto wanajua hata leo mtu anayekunywa pombe hawezi kuzungumza lugha asiyoijua na watu wa nchi hiyo wakaelewa. Vinginevyo ingekuwa rahisi kila asiyejua lugha fulani, anywe pombe ili asaidie kutafsiri lugha fulani. Siku hizi watu husema ukijua Kichina huwezi kukosa kazi, kwani kuna soko la lugha hiyo kwenye biashara nyingi. Basi watu wangekimbia wanywe pombe ili wazungumze Kichina wajipatie ajira kirahisi. Hata wachina wenyewe karibu wote wangependa wajue Kingereza, na wapo wengi karibu bilioni 1.5, na lugha yao ndiyo inazungumzwa na watu wengi kupita zote duniani, ikifuatia na Kingereza. Wachina wengi ninaokutana nao wangependa kuzungumza Kingereza pia.

Karama ya kunena kwa lugha ilitolewa kwa mitume ili injili iende duniani kote, kwani kwenye mnara wa Babeli lugha ziliongezeka zaidi ya ile moja kwa uasi. Kufikia

watu kwa ujumbe wa injili inakuwa kazi kama hatujui lugha zile. Kuna watu wana karama hii hata siku hizi. Aidha wanajifunza lugha kirahisi, au muujiza unatokea na wanajikuta wanazungumza lugha tofauti ili kufikia watu. Hata leo ahadi ya Roho Mtakatifu ni yetu wote. Hatuwezi kufanya kazi ya Mungu bila kumwagiwa Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu ni nafsi (person) tukiomba twapasa tujue hili. Katika maada ambazo Yesu alijikita akiwa duniani, ni kumwagiwa Roho Mtakatifu. Wengi tunaishi mahali penye watu wa lugha na jamii mbali mbali. Miji yetu Afrika imeingiliwa na watu wa mataifa yote, Wazungu, Wahindi, Waarabu, Wayahudi, Wachina, Wakorea, Waturuki na watu wa nchi mbali mbali. Wengi wa watu hawa hawamjui Kristo, wamekuja kwetu kutafuta maisha na nchi zao nyingi wamemwacha Mungu, ni jukumu letu kuwafikia kadri tuwezavyo. Wengine ni wakimbizi, wanafunzi wageni au watu waliokuja kutafuta vibarua katika nchi zetu. Scott Griswold ameandika kitabu 'Reach the World' yaani ufikie ulimwengu, nacho kiko bure mtandaoni, kisome hicho. Tuombe Mungu atupe njia za kufikia watu hawa, tusifikiri kwamba watu tunaozungumza lugha moja ndiyo wa kufikia. ReachtheWorldNextDoor.com
Rafiki aliyetoka Uturuki aliniambia alipata ukristo akiwa mtembeza watalii huko Uturuki, kutoka kwa Mkristo wa Afrika kusini aliyekuja kuvinjari, naye akawa anamwongoza kwenye sehemu zile za historia za Biblia kama pale Ararat safina ya Nuhu ilipotua na makanisa saba yale ya Ufunuo 2 na 3 ambayo yapo Patmo. Huyu mama aliamua kuwa mkristo kwa ajili ya kushuhudiwa na mtu huyu toka Afrika kusini tukawa naye shule pamoja kule Michigan. Nchi ya Marekani inapokea watalii 160 milioni kila mwaka, hii ni nusu ya raia wa Marekani. Mwanya huu ni nafasi nzuri ya kufikia watu wa mataifa karibu yote duniani. Mamilioni ya watu huja kwenye shule au biashara, watu ambao si rahisi kupata injili kwenye nchi zao. Tanzania inapata wageni milioni mbili kila mwaka, una nafasi ya kufanya kitu!
Mfano wale viongozi wa makampuni kama Honda ya Japani, wafanya biashara wa bidhaa za plastiki toka China, wataalamu wa Kompyuta toka India na nchi zingine ambazo hazimjui kabisa Mungu wa mbinguni, waweza kupokea injili wakiwa nchi za wengine. Hii ni nafasi ya Wakristo wa nchi hizo kutilia makini katika kufika watu; maana mara nyingi mtu akiwa kwenye nchi ya mwingine anapwaya, au kuwa mnyenyekevu kusikiliza. Mungu alisema kwenye Isaya 56 "Nyumba yangu itaitwaa nyumba ya sala kwa mataifa yote", na siyo taifa moja. Hata wale wanaopata nafasi ya kutembea nchi nyingine au kukimbia kule wamshuhudie Kristo kwa mataifa wasiyomjua. Na Sulemani aliomba Ombi hili katika ufunguzi wa hekalu "Vivyo hivyo wakati mgeni asiye mmoja wa watu wako Israeli atakuja kutoka nchi ya mbali kwa ajili ya Jina Lako kuu, na kwa sababu ya nguvu na ulinzi Wako, kuomba katika nyumba hii, nakusihi umsikie toka huko Kwako mbinguni, na umjalie huyo mgeni yote atakayokuomba kusudi watu wote ulimwenguni wapate kujua Jina Lako na kukutii kama wafanyavyo watu wako Israeli na wapate kufahamu kwamba nyumba hii ambayo nimeijenga inajulikana kwa Jina Lako."

Nchi zingine ni vigumu kuingia na injili, kwani wengi wameuwawa. Ila nchi hizi zina watu wanaotembelea nchi zetu kwa utalii kwenye mbuga zetu kuangalia wanyama ambao hawapo mahali pengine duniani, hawa wanaweza kukutana na Wakristo na kupewa habari njema. Je, ungependa watu hawa wapotee, na wasipate uzima wa

milele? Tuna watu wanaoabudu mizimu, na miungu mingine kama Hindu, Shinto, Confusius na Budha; kuna wengine hawaamini chochote, huitwa wapagani, na wengine wana dini za upagani (non religious).

Ombea hawa wote uweze kuwapenda. Omba Roho Mtakatifu, ombea na viongozi wa nchi ili milango ifunguke ya kushuhudia. Ombea madhehebu yote na Mungu kama Zaburi 67 inavyosema anataka "kuwapa wokovu watu wa mataifa na wote watamcha." Je kama wao wangejua habari za kuokolewa na kwenda mbinguni wasikuambie ungejisikiaje? Au kama ungejua dawa ya kutibu Korona, au Kansa au ebola na usimpe mtu, ingekuwaje? Injili ni dawa inayoponya ugonjwa mkubwa kupita yote, yaani dhambi, na kumwezesha mtu awe mbinguni siku moja! Tuombe kila siku ili tukue kiroho, na kusaidia wengine wamkubali Mwenyezi Mungu. Tuwe na umoja kwa kuondoa tofauti Tunapochunguza Neno Lake, na kisha kulitenda, nasi sote tutakuwa na nia moja na hubiri moja. "YESU NI BWANA, NA NENO LAKE NDIYO Mwongozo wa kila mtu."

Si lazima Roho aje kama ndimi ya moto, Roho wa Mungu hatumuoni ila kazi Zake zinaonekana. Yupo hata leo masaa 24. Yohana 16 yatuambia Roho Mtakatifu ni Mfariji, na Mwalimu wa kutufundisha mafundisho ya Mungu na imani, anatusaidia kuomba na kuugua kwa dua kwa ajili yetu. Anatukatisha shauri tumwamini Mungu na kutufanya dhamiri zetu zitushitaki ili tuone tunapotenda dhambi na tuungame. Hakuna anayeweza kuishi maisha ya imani bila Roho Mtakatifu. Ila twabidi tumruhusu Roho Mtakatifu awe kiongozi wa maisha yetu. Yesu asingeweza kuwa nao kila siku na kama asingeondoka Roho Mtakatifu asingemwagwa kwa wingi vile. Roho Mtakatifu tunaye wakati wote, mahali popote. Roho aja kwa kuomba, kusoma Neno la Mungu na kufunga, na kutennda maagizo ya Yesu, na hiyo itatusaidia kwenda dunia nzima.

Tunaambiwa kwenye kitabu cha Yoeli, siku hizi za mwisho mvua ya masika itamwagwa. Mvua ni Roho wa Mungu. Hata tukiwa wadhaifu tutawezeshwa na Mungu kufanya makuu, ni ahadi ya Mungu kwetu na watoto wetu. Leo katika kila nchi wamekusanyika watu wa kila kabila na jamaa, Wachina na Wahindi, ambao ni theluthi ya dunia, wamekuja kwa biashara Afrika na wengi hawamjui Mungu wa mbinguni. Hebu tuwafikie hata kwenye nchi zetu, maana Mungu anajali wokovu wao ndiyo maana Yesu akafa. Roho Mtakatifu atakuwezesha; anza na marafiki na wanafunzi wenzako.

*Kuchelewa kwa Kristo kwa siku mbili baada ya kusikia kwamba Lazaro alikuwa mgonjwa haukuwa upuuziaji au kukataa kwa upande Wake. Lilikuwa ni kusudi Lake kubaki pale alipokuwa mpaka kifo cha Lazaro kitokee, ili aweze kuwapa watu ushahidi wa Uungu Wake, sio kwa kumponya mtu anayekaribia kufa, bali kwa kumfufua mtu aliyezikwa tayari.

----------------------

Maswali: Nabii Yoeli anasema siku za mwisho itakuwaje? Kumwagiwa Roho Mtakatifu ina maana gani? Je, tunawezaje kumwagiwa Roho Mtakatifu? Je, Roho Mtakatifu anatusaidia mambo gani?

**SIKU YA 295.**
**(Oktoba 21)**

# Petro anahubiri.

**Matendo 2.**



Watu wakishangaa shangaa, ndipo Petro akainuka kwa ujasiri na kupaza sauti akasimulia kisa cha wokovu chote akisema "Enyi watu wa Uyahudi na wote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, siyo kama mnavyoamini, hatukulewa sisi, maana ni saa tatu asubuhi, ila jambo hili limetokea kutimiza Maneno ya nabii Yoeli akisema Nitawamwagia watu wote Roho Yangu na wana wenu na binti zenu watatabiri na vijana wenu wataona maono, na wazee wenu wataota ndoto, na ishara za mbinguni zitaonekana kama jua kutiwa giza na mwezi damu, kabla ya kuja ile siku ya BWANA…. na itakuwa kila atakayeliita Jina la BWANA ataokolewa"

Hii ilikuwa ahadi ya Mungu kwao na kwetu na watoto wetu leo. Petro akazungumza habari za Yesu wa Nazareti alivyofanya miujiza na ishara na jinsi walivyomsulubisha na Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti …..Daudi alimwona mbele yake Masihi siku zote… akapaa juu mbinguni na anakaa mkono wa kuume wa Mungu Baba… basi Nyumba yote ya Israeli wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu Huyo mliyemsulubisha kuwa BWANA na Kristo."Watu waliposikia mahubiri ya

Petro ya ujasiri, walichomwa mioyo yao, maana walihusika na kufa kwa Yesu, hata Pilato Mrumi aliwashangaa walivyokazana Yesu afe. Waliishi maisha ya dhambi kama binadamu wote, ila walijua ni saa ya kupokea toba ya Kweli na wakajutia.

Petro alihubiri bila daftari, kipaza sauti au Projekta, ila watu walibadilishwa. Watu wakawaambia mitume "Tutendeje ndugu zetu?" Petro akawaambia wajirudi na kuanza upya "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa Jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Ahadi ya Roho Mtakatifu ni yetu leo na watoto wetu pia, na wote walio mbali ambao BWANA anawaita na wanakubali wito Wake. Petro akawashuhudia maneno mengi na kuwaonya wajihadhari na kizazi chenye ukaidi. Nao waliposikia maneno yale wakabatizwa siku zile wapata watu 3,000. Yawezekana hii ilikuwa idadi ya wanaume tu, na hii ndiyo ikawa mbegu ya kanisa la Kikristo la kwanza. Wengine ni wale waliokuwa hawajamwamini Kristo akiwa anaishi, bali kwa vile Kristo alisema "nikiinuliwa nitawavuta wote Kwangu."

Watu walianza kuvutwa kwa Yesu, hata leo sisi tumevutwa Kwake. Yesu anayetupenda akatufia kwa kuinuliwa msalabani, na kisha akafufuka, hata leo, Naye ana uwezo wa kutuondolea dhambi zetu na kutusaidia tuishi maisha ya utakatifu. Wakawa wakidumu pamoja kama ndugu katika Mafundisho ya mitume na katika ushirika na katika kuumega Mkate na katika kusali. Kila mtu akaingiwa hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume. Watu wote walioamini walikuwa mahali pamoja na vitu vyote vikawa shirika, wakiuza mali zao na vitu vyao walivyokuwa navyo na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na mahitaji. Hakuna aliyehitaji au kupungukiwa.

Siku zote moyo wao ulikuwa mmoja wakishikamana, walidumu kwenye hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe uliotakata bila hila, chuki, wivu au kiburi; wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote. BWANA akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa. Kama vile Yesu alivyosema ndugu Zangu ni wale wanaoshika mafundisho Yangu, basi hawa wafuasi wa Yesu wakawa ndugu za Yesu. Na waumini wakawa kaka na dada wa kila mmoja wao. Si kwamba Yesu hapendi tukae karibu na familia zetu, la hasha. Miaka mingi kabla Yesu hajazaliwa Mungu alitoa Amri "Waheshimu baba yako na mama yako."

Yesu anataka tuwapende na kuwaheshimu wazazi wetu, na ndugu pia. Wazazi na watoto wanaishi pamoja kwa muda, kisha kuna siku watoto waenda kujitegemea, wakiendelea na maisha yao wenyewe. Uhusiano wao ukiendelea kuwa mzuri, wanasaidiana katika shida na raha. Na pale wanapopata ndugu na jamaa katika Kristo au wa familia ya Mungu, wanatiana moyo na kusaidia katika shida na raha pia. Wanatiana moyo katika kutembeleana katika hii familia mpya ya Kristo. Mara zingine yaweza kuwa ni ya karibu sana kuzidi ndugu wa damu. Ni Kweli kwamba wazazi na watoto ambao wana imani moja katika Yesu wanakuwa karibu zaidi kuliko familia za kawaida.

Nuhu alikuwa na familia ya namna hii, japo hakuokoa wengine, walakini aliokoa familia yake, maana walimsikiliza na kufanya kazi ya Mungu pamoja na watoto wake huku wakimtii. Mfano huu ndiyo bora kupita yote, ila endapo hauna zawadi hii ulipozaliwa, usikate tamaa, maana una jamaa mamia kwa imani uliyopokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kupitia Mwana Wake Yesu Kristo. Tunachopaswa kukumbuka ni kwamba kupenda familia yetu, kusiingiliane na kumtii Mungu. Tukumbuke tumeumbwa wote na Mungu na hivyo wote tu familia ya Mungu, kisha tukanunuliwa Naye kwa damu ya thamani.

Kitabu cha Matendo hujaza moyo wangu furaha na matarajio kupita kitabu kingine chochote kwenye Biblia. Ninaona ndani yake, picha wazi ya kile kinachokuja kuhusu kumwagwa kwa mvua ya masika ya mwisho. Luka, mtaalam wa kihistoria, aliandika Matendo akiwa anasafiri na Paulo. Kabla ya Yesu kupaa mbinguni, aliwapa wafuasi Wake ufunguo muhimu sana ambao ungewawezesha kutimiza Utume wetu Mkuu. Yesu aliwaamuru wanafunzi Wake hawapaswi kuondoka Yerusalemu, lakini wasubiri ahadi ya Baba : "Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Uyahudi kote na Samaria, hadi miisho ya dunia "Kristo ametupa Utume mkuu wa kuchukua Injili Ulimwenguni kote, lakini ni mara ngapi katika shauku yetu tunafanya dhambi kubwa ya kuacha kutenda mambo mengine (omission). Twapaswa tuungame dhambi zetu na kuwa na umoja. Neno la Mungu lasema daima tupige magoti yetu tukiomba nguvu Zake. Nataka Yesu aje leo, lakini hata ikiwa hatakuja katika maisha yangu, jambo moja ni la hakika ni kwamba Yeye atakuja tena. Atakuja tena kuchukua watu Wake nyumbani siku moja, hiyo ndiyo motisha tunayohitaji ili kufanya wakati wa maisha yetu tayari katika kuuandaa ulimwengu kwa Yule anayekuja. Siku moja, ulimwengu wetu huu mbaya utafikia mwisho. Hivyo katika pande ya dunia tulipo, tuandae ulimwengu kwa kuja Kwake Bwana. Hakuna sababu nyingine yenye stahiki kuliko hii! Mungu asema "Uzishike nguvu zangu, Ufanye amani Nami; Naam, afanye amani Nami." Yeye atatusaidia, ila hatupaswi kujitenga na kukaa wenyewe saa zote, nuru yetu inapaswa kuangaza, ili watu wamwone Mungu. Wakati adui anacheza mchezo na maisha ya watu, hatupaswi kuyaacha chini makasia, tunapiga makasia kuelekea juu, na mara nyingine kuna upepo wa mbisho, hivyo inabidi tuyatumie tuweke bidii zote.

*Katika maisha ya baadaye mafumbo na siri ambazo hapa zimetukasirisha au kutupa usumbufu na kutukatisha tamaa zitawekwa wazi. Tutagundua kwamba maombi yetu yaliyoonekana kutokuwa na majibu na matumaini na yaliyotukatishwa tamaa, hayo yamekuwa miongoni mwa baraka zetu kubwa.
-----------------------------

Maswali: Petro alisema nini kwenye mahubiri? Kwa nini watu waliguswa mioyo? Kwa nini mitume walidumu kwenye mafundisho na ushirika? Je, mtu anawezaje leo kudumu katika mafundisho ya Mungu akiwa kwenye ushirika? Mitume wanatupa fundisho gani la maana kuhusu kujiunga na ushirika?

**SIKU YA 296.**
**(Oktoba 22)**

# Kiwete aruka ruka.

**Matendo 3**



Mbali na kuzungumza lugha tofauti nyingi, na kuwa wahubiri mashuhuri, mitume walipewa uwezo wa kuponya. Yaani walikuwa zaidi ya madaktari. Pia walisaidiwa kutoa Pepo na miujiza mingine ya aina mbalimbali ilifanyika. Watu wengi sana walipewa kufanya kazi ya Yesu. Kazi hii hata sisi, yaani mimi na wewe tumepewa leo tuendelee nayo, maana Paulo, Petro, au Yohana hawapo, ni sisi tumepokezwa mwenge huu au kijiti hiki, basi yabidi tukimbie nacho kwa uwezo Wake Mungu.

Siku moja, Yohana na Petro walikwea saa tisa hekaluni kusali, na mtu mmoja aliyekuwa kiwete toka tumboni mwa mamaye alikuwa amechukuliwa na watu wakimweka kwenye lango la hekalu liiitwalo Mzuri, ili aombe sadaka kwa watu waingiao ndani ya hekalu. Kwenye miji yetu mingi tumewaona watu wa namna hii na kuwapa majina ya "omba omba." Mtu huyu alipowaona Petro na Yohana wakiingia hekaluni aliwaomba sadaka, naye Petro akamkazia macho, pamoja na Yohana wakamwambia "Tutazame sisi", naye akawaangalia akitaraji kupata kitu, ndipo Petro akasema "Mimi sina fedha wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho, nacho ni cha thamani zaidi, Kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende."

Akamshika mkono wake wa kuume, akamwinua, na mara nyayo zake na vifundo vya miguu yake vikatiwa nguvu. Akaondoka upesi, akasimama, akaingia ndani ya hekalu, akiruka ruka na kumsifu Mungu. Watu wote wakamwona akienda akimsifu Mungu, wakamtambua ndiye yule omba omba aliyeketi kwenye mlango Mzuri wa hekalu, wakastajaabu kwa mshangao, mambo yaliyompata.

Alipokuwa akiwashika Petro na Yohana kuwashukuru, watu waliwakusanyikia mbio katika tao lilioitwa la Sulemani, wakishangaa sana maana walimjua toka udogo. Pengine ndugu zake walimbeba na kumweka mahali wazi wapitapo watu ili aombe pesa. Ndipo Petro akasema "Enyi Waisraeli mbona mnastaajabia haya, mbona

mnatukazia macho sisi, kana kwamba tumemponyesha mtu huyu kwa nguvu au utakatifu wetu sisi?" Wakawaambia "Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo wa baba zetu amemtukuza mtumishi Wake Yesu, Ambaye ninyi mlimsaliti na kumkana Yule mtakatifu, na Mwenye haki mkataka mpewe mwuaji Baraba, mkamuua na Mungu amemfufua katika wafu na sisi tu mashahidi Wake. Na kwa imani ya Jina Lake Yesu, limemtia mtu huyu nguvu kilema alicho nacho kikatoweka."

Akaendelea kuhubiri akiwaambia "Ndugu najua mliyatenda maovu yale kwa kutojua kama wakuu wenu walivyotenda, lakini mambo yale aliyohubiri Mungu tangu zamani, kwa kinywa cha manabii Wake wote ya kwamba Kristo atateswa yametimizwa hivyo tubuni basi mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako Kwake BWANA, apate kumtuma Kristo Yesu mliyepewa tangu zamani. Mungu aliwaambia atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama Mimi msikieni na mambo yote atakayonena nanyi.

Akawaambia ni kweli watu waovu watawaangamiza na kuwatenga wasipomsikiliza huyo nabii. Ibrahimu aliambiwa katika uzao wako kabila zote za ulimwenguni zitabarikiwa. Mungu alipomfufua katika wafu Yesu alimtuma kwenu ninyi ili kuwabarikia kwa kumwepusha kila mmoja wenu na maovu yake.

Hata leo nasi tumetumwa kuhubiri habari njema za ujumbe huu wa uponyaji kwa vilema, na watu wote duniani ujumbe huu "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja. Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:7. Ujumbe huu ni muhimu sana wakati huu wa mwisho zaidi hata ya wakati ule wa mitume, na tusiruhusu kitu kingine kugeuza umakini wetu. Tunahubiri ujumbe wa malaika wa kwanza "akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi" (Ufunuo 14:6), akiwasihi wote kumcha Mungu, kumtukuza, na "kumsujudia Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji" (fungu la 7). Mafungu haya hutukumbusha kwamba chimbuko la ubinadamu ni Mungu, Yeye ndiyo Muumbaji, na wala siyo uibukaji. Sisi tunaoamini Neno Lake tuna "injili ya milele" injili ya wakati husika, isiyopimika, muhimu, ya milele, inayohitajika na isiyo na mwisho. Pia tunashiriki ujumbe wa malaika wa pili unaopatikana katika Ufunuo 14:8: "Umeanguka Babeli!" Ujumbe huu mtakatifu unawataka wafuasi halisi wa Mungu kukataa aina zozote za ibada na imani za kibinadamu zisizojengwa katika Neno la Mungu. Hutuita tutoke katika Imani zilizokusanywa kiholela ambazo hazijajikita katika Maandiko wala hazitegemezwi na Roho ya Unabii. Malaika wa Ufunuo 18:4 anaagiza baadaye kuwa, "Toka Babeli, usishiriki dhambi zake wala usipokee mapigo yake." Ujumbe huu mtakatifu ni wito wa kusimama imara katika ibada yetu ya Kweli kwa Mungu!

Ujumbe wa malaika wa tatu unagusa injili ya ujumbe wa kwanza na wito wake wa ibada! Hubeba wito wa ujumbe wa malaika wa pili wa kujitenga na ibada ya uongo. Lakini jinsi ya kutangaza ujumbe huu wa tatu si kama ule wa kwanza na wa pili kwani huu unawasilisha onyo la kutisha zaidi, ukisema: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya

Mungu iliotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira Yake" (Ufunuo 14:9). Ujumbe huu unadhihirisha watu wa dunia wanaomwabudu mnyama na kupokea chapa yake na wanaomwabudu Mungu waliotiwa muhuri wa mbingu! "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu" (Ufunuo 14:12). Ujumbe huu ndiyo wa kuhubiriwa sasa. Ujumbe huu unapaswa kwenda na nguvu kubwa iliyo tofauti kabisa. Haupaswi kufunikwa na nadharia na madanganyo ya kibinadamu Kadiri tunavyoomba leo, tumuombe Mungu atie nguvu ibada zetu ili tuweze kutangaza kwa nguvu ujumbe Wake wa wakati wa mwisho kwa dunia inayoharibika.

Tukumbuke kwamba kila mmoja wetu ana sababu ya kurukaruka na kumsifu Mungu! Tunaye Mwokozi, Yesu Kristo Bwana wetu. Tumekombolewa! Tuna tumaini la milele! Jipeni moyo marafiki zangu. Usiangalie chini. Usiangalie tu shida zako. Inua kichwa chako leo. Mtafute Yesu; Tazama juu. Yesu Ndiye Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu. Hebu leo tutembee na kurukaruka na kumsifu Mungu kama yule kilema!

Unasema nini?
Ombi: Mungu Muumbaji wetu mkuu, Mfalme wa Ulimwengu, tunataka kujinyenyekeza katika uwepo Wako. Wewe ni Mungu wetu, Mungu pekee, na unastahili sifa zetu, ibada zetu, na maisha ya kujitoa kwa mapenzi Yako. Wewe ni wa ajabu, Mwema, mwenye nguvu. Tunaomba uweze kutimiza ahadi Yako na kutujaza na Roho Mtakatifu ili maisha yetu yaakisi tabia Yako kamilifu ya upendo. Tunaomba ujitukuze na kujidhihirisha kupitia kwetu. Tunajua tunaishi katika saa ya hukumu ya historia ya dunia. Asante kwa kuwa umetupa ujasiri katika utoshelevu wa haki yako, ambayo ni yetu kwa Imani, na inayotupatia uhakika wa wokovu kadiri tunavyoikabili hukumu. Tusaidie, kwa neema Yako, kuishi maisha ya huduma yenye faida, yaliyojikita katika utume, tukikuheshimu katika yote tunayotenda. Licha ya madhara ya dhambi, bado tunaweza kuona kwamba Wewe Ndiye Mbunifu Mkuu aliyeweka uzuri mwingi katika kazi za mikono Yako. Tusingekuwepo bila Wewe. Asante kwa kushiriki maisha Yako na kutuumba, si tu tuwepo kwa ajili yetu wenyewe lakini tuishi katika ushirika wa milele pamoja na Wewe, Muumbaji wetu. Kwa Jina Lako tukufu, Amina.

*Lile Ombi la dhati litokalo moyoni kwa bidii na Imani lina ufanisi, usiochoka, wenye manufaa, na msaada wa hali ya juu. MUNGU hajibu maombi yetu kila mara kama sisi tunavyotarajia, kwani tunaweza tusiombe kile kilicho bora zaidi kwetu; bali kwa upendo na hekima Yake isiyopimika, Yeye atatupatia vile vitu ambavyo ndivyo tunavyovihitaji sana.
--------------------------

Maswali: Kwa nini kuponywa kwa kiwete ilikuwa muhimu kuliko kupata fedha au dhahabu? Wayahudi walitenda maovu bila kujua, Je, sisi tunatenda bila kujua pia? Kwa nini watu walimkazia macho Petro? Hakuna wokovu isipokuwa kupitia Jina gani? Je, tunawaambia wengine Neno la Uzima? Je, unaamini miujiza ya Mungu? Kariri malaika waatatu wanasemaje? Utajuaje kwamba una ibada ya uongo? Je, unasoma Maandiko kila siku?

**SIKU YA 297.**
**(Oktoba 23)**

# Mitume wanaingia Gerezani kwa mara ya kwanza.

**Matendo 4.**



Wakiwa katika kuhubiri makuhani ambao wengi walikuwa masadukayo, na maakida wa hekalu wakawatokea wakifadhaika maana walikuwa wakihubiri kuhusu ufufuo wa wafu, wakawakamata na kuwaweka gerezani hata asubuhi kwa kuwa imekwisha kuwa jioni. Masadukayo hawakuamini ufufuo au malaika. Injili ni habari njema ya Yesu kufa kwa ajili yetu na kufufuka kama kuhani wetu ili atuombee. Basi masadukayo waliipiga vita injili hii, kwa ajili ya imani yao. Ila baadaye makuhani wengine waliamini.

Japo waliwashika baadhi ya watu; wengi walikuwa wamesikia Neno. Basi watu wapata watu 5000 walimwamini Yesu. Hata asubuhi wakuu wa waandishi na wazee walikusanyika Yerusalemu. Na Anasi kuhani mkuu, Kayafa, Yohana wa Iskanda na wote waliokuwa jamaa ya kuhani mkuu wakawauliza "kwa nguvu gani na kwa jina la nani mnafanya haya?" Ndipo Petro akijaa Roho Mtakatifu, akawaambia bila hofu,

na kwa heshima, Enyi wakubwa wa watu na wazee wa Israeli, kama tukiulizwa leo habari ya jambo jema la kupona yule kiwete, jueni ninyi na watu wote pia wa Israeli ya kuwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti Ambaye ninyi mlimsulubisha na Mungu akamfufua katika watu, kwa Jina hilo la Yesu, mtu huyu anasimama mzima mbele zenu. Yeye Ndiye jiwe kuu la pembeni. "Hakuna wokovu kwa Jina lingine lolote chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo isipokuwa hilo." Petro alipata muda tena na tena wa kumshuhudia Bwana, Mungu aliwapa mimbari za kushuhudia pengi. Hata leo Mungu anatupa nafasi, tumwombe ili tugundue na kuzitumia nafasi hizo. uhitaji kwenda chuo cha uchungaji kwanza ili ushuhudie, unaweza kuwa mlei, ila sali na soma Maandiko ya Biblia, nawe utashangaa utakavyoweza kuwafikia wengi. Ila ukipata wito wa kwenda Seminari ili uwe mchungaji na kisha uwafundishe wengine kufikia watu kwa njia fulani, nalo ni jambo bora kabisa. Yesu ni njia yetu ya kwenda mbinguni, bila Mkombozi, hakuna awezaye kuokolewa. Yeye ni Kweli, bila Yeye tutaishi kwenye Uongo. Yesu ni uzima, bila Yeye hakuna maisha. Makuhani masadukayo walifikiri njia yao au mapokeo ndiyo kweli, bali ilikuwa ni uongo. Yesu ni uzima, bila Yeye hakuna awezaye kupata uzima wa milele. Twaweza kupata njia, Ukweli na uzima tu, tukiwa na umoja ndani ya pendo Lake. Tukiamini na kumfuata Yesu na Mafundisho Yake daima tutakuwa watu wenye furaha na amani, hata mambo yakienda mrama.

Wale makuhani, masadukayo na wazee walipoona ujasiri wa Petro na Yohana na wakijua ni watu wasio na elimu, na maarifa maana hawakwenda shule za kawaida au za msingi, walistaajabu, wakatambua kwamba zile akili na hekima nyingi zimetokana na kuishi na Yesu. Yesu aliwapa uwezo ule. Na hata wewe leo, ukitaka uwe na uwezo darasani, maamuzi ya busara, uvumbuzi, na kuishi na watu vyema, uwe unakaa miguuni pa Mungu na utajifunza mengi ya muhimu mno. Hata wale waliokuwa na shahada za juu watakuwa hawana uwezo wa kujiamulia mambo ya maisha yao kama wewe japo u mtoto. Hii ni kwa sababu busara zako zitatoka kwa Mwenyezi Mungu.

Wakamwona yule kiwete aliyeponywa yupo pamoja nao, ikawa ni ushahidi tosha, kuwafunga vinywa kwa aibu. Walipohojiana wawafanyie nini watu hawa, maana watu wote wa Yerusalemu mji ule mkuu waliona ishara, hivyo wasingeweza kukana kama hakuna jambo hilo, au kwamba halikutokea. Basi wakawaita na kuwatisha-tisha "msiseme kabisa wala kufundisha kwa Jina la Yesu." Petro na Yohana wakasema kwamba Je ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu? Wakasema wao hawawezi kuacha kuyanena yale waliyoyaona na kuyasikia kwa ajili ya ukombozi. Basi waliwatisha tisha tena na kuwafungua, wasione njia ya kuwaadhibu, kwasababu watu wote walikuwa wakimtukuza Mungu kwa hayo yaliyotendeka, yaani kiwete wa muda mrefu wa miaka 40.

Walipofunguliwa walienda na kuwaambia yale waliyoambiwa na wale makuhani na wazee. Wakamwomba Mungu wakisema "mbona mataifa wanafanya ghasia. . . na wakuu wanafanya pamoja shauri juu ya BWANA na juu ya Kristo Wake." Wakamwomba Mungu aangalie vitisho wanavyopata na kuwajalia kunena Maneno ya Mungu kwa ujasiri; na kuwasaidia kuponya watu na maajabu na ishara yafanyike kwa Jina la mtumishi Wako mtakatifu Yesu. Wakimaliza kuomba tu hivi, mahali pale

pakatikiswa na Roho wa Mungu, na wakajazwa Roho Mtakatifu tena na wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri. Wengi wakaponywa, wakaendelea kuhubiri, kwa ujasiri wasijali vitisho.

Jamii ya hawa watu walioamini walikuwa na moyo mmoja, na roho mmoja, hakuna aliyesema ya kuwa kitu hiki ni mali yangu mwenyewe, bali walikuwa na vitu vyote kama shirika moja. Mitume wakaendelea kushuhudia maisha, na kufufuka kwa Yesu na neema nyingi ikawa juu yao wote. Hapakuwa na mwenye hitaji, kwani walisaidiana. Watu waliuza viwanja au nyumba na wakaleta ile fedha na kuweka miguuni pa mitume, na kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji. Naye Yusufu, aliyeitwa Barnaba au Mwana wa matumaini, ambaye alitoka kisiwa cha Kupro, aliwafariji wengi na kuwasaidia kwa ucheshi wake. Alitumia muda wake, mali na talanta zake, kuhudumia watu na Mungu. Akajulikana kwa jina la mwana wa matumaini! Wana wa matumaini wanatakiwa kila mahali, iwe shuleni, nyumbani, kazini au katika jumuiya kwani wanatia watu moyo au shime. Kila mtu ana talanta ya wakati, hebu tutumie muda wetu kunena maneno ya kuponya kwa watu na si ya kufisha. Daima tuwape watu matumaini yaliyo ndani ya injili.

Barnaba alimtolea Mungu sadaka kubwa kutoka moyoni mwake. Tunajua katika matoleo yetu kwa Mungu kuna sadaka, na kisha zaka. Mtunga Zaburi anasema nimrudishie nini Bwana kwa ukarimu Wake alionitendea Zaburi 116. Akagundua kwamba hawezi kumrudishia chochote cha maana, maana Mungu anamiliki kila kitu mbinguni na duniani, hivyo akasema atazitimiza nadhiri zake, atakipokea kikombe cha wokovu, na kuwasilimua watu matendo ya Bwana kama shukurani zake kwa Mungu. Zaka ni asilimia 10% ya mapato mtu anayoyapata. Sadaka ni kiasi chochote mtu anataka kumtolea Mungu wake, mara nyingi mambo yakiwa mazuri sadaka huwa ni kubwa kuliko zaka. Watu husema kwamba asilimia 90 ya mali walizo nazo watu haziko katika mfumo wa fedha, ambao unaweza kuzunguka, yaani nyumba na vitu walivyo navyo (si cash flow). Barnaba alikuwa ni mtu mkarimu, hakutoa ili ajionyeshe, bali asaidie kazi ya Mungu. Sadaka zinazotolewa zaweza kuwa sadaka za shukrani, sadaka za kusaidia masikini, sadaka za baraka au afya. Kusoma Maandiko, kuomba, kuimba, na kutoa zaka na sadaka ni sehemu ya ibada kwenye Maandiko. Hivyo Mungu anapotubariki, tusije mikono mitupu kwenye ibada tunapokuwa na mapato! Maana Yesu alisema pale hazina zetu zilipo, ndiyo moyo wetu ulipo, na siyo pale moyo wetu ulipo ndiyo hazina zetu zilipo! Endapo una mamilioni ya pesa ndani ya kabati nyumbani mwako, mawazo yako yatakuwa hapo, basi tutafute jinsi ya kuweka hazina zetu mahali pazuri ili mioyo yetu iwe huko. Mbinguni ni mahali pazuri kuweka hazina zetu!

Tunapokabidhi pesa “zetu” kwa Yesu, kwa hakika huimarisha upendo wetu Kwake na kwa wengine. Fedha zetu zinaweza kutenda mema mengi. Yesu alitumia muda mwingi kuzungumza juu ya pesa na mali kuliko somo lingine lolote. Mstari mmoja katika kila sita katika Mathayo, Marko, na Luka unahusu pesa. Habari njema za Injili ni kwamba Mungu anaweza kutukomboa kutoka kwa matumizi mabaya na kupenda pesa. Usitoea pesa zako kwasababu ya uzee au ukifa watu walete kanisani, toa ukiwa na afya yako nzuri.

Matoleo yetu ni ushahidi wa utayari wetu wa kujitolea kwetu kwa Mungu. Mara zingine huonyesha kuwa maisha yetu yamekabidhiwa kikamilifu kwa Mungu kama Bwana wetu. Unaweza kusema unampenda Mungu, lakini matoleo ya ukarimu husaidia kufichua na kuimarisha upendo huo. Unapotoa zaka au sadaka kumbuka ile kafara ambayo ilitolewa kwaajili yako. Sadaka ni tendo la ibada. Sadaka za aina tofauti, iwe hata kutumia muda wako, hutiririka kutoka kwenye moyo ambao umemkubali Kristo na kukiri na kuonyesha shukrani zetu kwa Mungu kwa ajili ya zawadi Zake. Mungu ametupa vingi, na tunapotoa, tunamrudishia vile alivyotupa tu.

*Katika Maombi Tunahisi Uwepo wa Yesu — Iwapo tutamweka Bwana mbele yetu daima, tukaruhusu mioyo yetu kwenda kumshukuru na kumsifu, tutafanywa upyakatika maisha yetu ya kiroho. Maombi yetu yatakuwa katika mfumo wa mazungumzo na MUNGU kama ambavyo tungezungumza na rafiki. Atazungumza nasi kuhusu mafumbo na siri Zake. Hisia nzuri za shangwe ya uwepo waYesu zitatujia mara kwa mara.
----------------------------

Maswali: Hakuna wokovu kwa Jina lolote duniani isipokuwa la nani? Jamii ya wale walioamini walikuwa na umoja wa namna gani? Kijana kiwete alikuwa na umri gani? Kwa nini mitume walikuwa na ujasiri na elimu ya juu iliyowashangaza watu? Kwanini ni muhimu tukiwa na mapato tutoe sadaka? Je, mtu awezaje kuwa mwana wa matumaini? Sadaka hutumiwa kufanyia nini?

**SIKU YA 298.**
**(Oktoba 24)**

# Anania na Safira.

**Matendo 5.**



Mitume hawakumlazimisha mtu kuleta mali zake, au kuziuza, bali waumini hawa waliona kwamba itasaidia wakiwa na ushirika mmoja na kufanya kazi ya kuhubiri habari njema ili kila kiumbe aipate. Wale waliokataliwa na kufukuzwa na ndugu zao, au waajiri wao, walifaidika pia kutoka kwa ndugu wa imani. Waumini walikuwa na furaha kufanya hivi, hakuna aliyewaambia wafanye. Hili lilifanya kazi ya Mungu ienee kama moto kwenye majani makavu kwa sababu ya kujiota huku. Ushirika huu uliwasaidia wale wote walio na mahitaji, hivyo hakuna aliyelala njaa, aliyekosa nguo au pa kulala. Kuamua kutoa mali yake mtu huyo, ilikuwa nadhiri yake ya hiari kwa Mungu na si kwa binadamu.

Basi mtu mmoja aitwaye Anania na mkewe Safira waliokuwa kwenye ushirika huu waliouza mali zao, na kuweka nadhiri watatoa kila kitu ili isaidie kueneza injili; walificha sehemu, na kuleta fungu jingine kwa ajili ya tamaa na kutaka wadhifa au sifa ya ukarimu. Alitangulia Anania, na kuweka miguuni pa mitume fedha, akisema kwamba ameleta kila kitu. Shida hii huwa inatokea kwa mtu anayetaka kujionyesha kwamba anatoa sadaka nyingi, ila ndani ya moyo wake hana ukarimu huo. Watu waliotoa mali zao walikula na kutegemea kusaidiwa mahitaji yao na ushirika wao. Anania na mkewe, walitaka wapate mafungu yote, walichobakiza nyumbani na kile cha ushirika. Walitaka umaarufu wa kujulikana kuwa wakarimu waliotoa yote, bali waliweka vibindoni vingine.

Petro akivuviwa na Roho Mtakatifu alielezwa kilichokuwa kinaendelea. Anania bila kujua Roho ameshawambia mitume Petro alipomwuliza, ni yote mali hii uliyouza shamba lako?, alisema “ndiyo.” Petro alimjibu “Anania, Kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja? Kabla hujaamua kuuza kiwanja au kutoa nadhiri, ilikuwa mali yako. Kama ungeuza bila kumwahidi Mungu, Je, pesa haingekuwa yako kuitumia unavyopenda? Ila ulipomwambia Roho Mtakatifu kwamba utatoa yote, umesema uongo na sasa si kwetu bali na kwa Mwenyezi Mungu.” Anania aliposikia maneno haya alipata mfadhaiko, na akaanguka, na kufa. Hofu nyingi ikawapata watu waliyosikia haya. Vijana wakanyanyuka na kuchukua ule mwili na kuuweka kwenye

sanda. Wakamchukua na kumzika, pengine bila familia yake kuwa na habari.

Baada ya masaa matatu kupita, akaingia mke wake naye hana habari ya yaliyotokea, asijue kwamba yeye sasa ni mjane kwa masaa matatu, akaenda kumwona Petro. Pale aliulizwa "Mama niambie, mlikiuza kiwanja kwa thamani hiyo kama mume wako alivyosema." Safira akaitikia ule uongo, akiwa upande wa uovu na mume wake "Ndiyo." Basi Petro akamwambia "imekuwaje wewe na mume wako mkapatana kumjaribu Roho wa Mungu kwa ulaghai, angalia miguu ya wale waliomzika mume wako ipo mlango hapo nao watakuchukua nawe nje kukuzika." Mara hiyo Safira akaanguka miguuni pake na akafa, wale vijana wakaingia wakamkuta amekufa, wakamchukua nje wakamzika pamoja na mumewe. Watoto wao walipata huzuni mno, pengine walijifunza kwa mfano wa kupoteza wazazi wawili siku moja, kutosema uongo kwa Mungu. Hata leo twapasa kuwa waaminifu kurudisha zaka, na kutoa sadaka Mungu anapotupa, na nadhiri au ahadi tunazompa Mungu si mchezo au jambo la mzaha. Mungu Hadhihakiwi, lolote apandalo mtu huvuna hatuwezi kupanda bangi na kisha tukavuna majani ya kunde.

Hofu nyingi ikawapata kanisa lote na watu wote waliyoyasikia ikawasaidia kuacha tabia za kumdanganya Mungu. Walielewa kwamba mtu aweza kufa kwa kusema uongo, na si kwa panga wala, mkuki. Anania na Safira walikumbwa na tamaa na kuona wanatoa nyingi, basi wafiche nyingine na kusema uongo. Wakafikiri watatumia kununua nguo, na vitu vizuri walivyovipenda. Wakazungumza na kupatana kwa uovu. Hata leo si vyema mke na mume, au wazazi na watoto kupatana kwa mambo yasiyo na haki. Umoja wa waumini Yesu aliosema, ni umoja kwa vitu vyema. Bwana na bibi Safira walifikiri, Petro atawashukuru kwa kuwasaidia na pesa, wasijue wanamchukiza Mungu. Yawezekana kabisa, Petro alionywa na Roho wa Mungu kuhusu maisha ya mtu huyu na mke wake.

Mungu akawatumia mitume kufanya miujiza na ishara nyingi, na kuponya watu. Waumini walikuja pamoja kuomba kwenye ua wa Sulemani karibu na hekalu. Ila viongozi wa Wayahudi hawakuthubutu kushughulika na mitume, wakiona aibu kuonekana nao, japo mitume waliendelea kuthaminiwa kwa hali ya juu na watu. BWANA akaongeza waumini wengi wanawake na wanaume. Petro aliwaponya kwa Jina la Yesu Mnazareti. Hata walio na pepo wakaponywa.

Kanisa lilianzishwa na Kristo – Bwana aliteua viongozi wake wa kwanza (Mk. 3:14) Naye analipenda kanisa Lake kama Bwana harusi ampendavyo bibi harusi wake. Wakati Petro anazungumza na Anania na Safira, alizungumza kwa niaba ya Kanisa. Pale penye utesi kawaida kanisa halifanyi kazi zake waziwazi hivyo watu hukutana majumbani, kama nyuki ili wafanye kazi vyema lazima wawe na mzinga. Ila hapa Petro akiwa na mitume waziwazi , na viongozi wenzake na washiriki wa kawaida anafanya shuguli ya kanisa, ili kuliboresha kanisa. Alionyeshwa kwamba anakuja mtu na mkewe, nao ni walaghai. Kanisa ni nini? Biblia hutumia vielelezo vingi kuwakilisha kanisa, taifa takatifu, watu wa agano, mwili wa Kristo, familia ya Mungu, kaya ya imani, bibi harusi wa Kristo, ukuhani wa kifalme. Kanisa mahalia humaanisha kusanyiko la watu. Je vyote hivi humaanisha nini? Kanisa ni nini hasa? Kanisa ni kundi la watu Wakristo. Kanisa ni kiumbe hai ambacho Kristo Mwenyewe

hukipatia uhai wa kiroho. Kwa hiyo haiwezi kufasiliwa kwa maneno ya kibinadamu tu. Kwa hali yoyote, ni muhimu kuliona kanisa kama lililojengwa katika Kristo na lenye kushughulika na watu. Kanisa halipo kwa ajili yake lenyewe kama asasi bali kwa ajili ya watu wake. Kanisa ni kundi la watu. Neno Kanisa wakati mwingine hutafsiriwa kuonesha watu walioitwa ili watoke, waliotengwa ingawa ni kweli kwamba Wakrsto wameitwa kutoka katika ulimwengu, wameitwa ili wawe pamoja. Ukristo ni dini ya mahusiano na siyo upweke. Kanisa si jengo ambapo kundi la watu hukutana bali kundi la watu wanaokutana kwenye jengo. Kanisa ni kundi la watu Wakristo walioitwa ili watoke katika ulimwengu, na wanaojifunza kumpenda Mungu na kupendana wao kwa wao.

*Tunapaswa kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu kama walivyofanya Wanafunzi katika Pentekoste — Moyo lazima ukungutwe kila punje ya unajisi na kusafishwa kwa ajili ya kukaa kwa Roho. Ilikuwa kwa kuungama na kuacha dhambi, kwa kuomba kwa dhati na bidii na kujitoa wakfu kikamilifu wenyewe kwa MUNGU, ndivyo wanafunzi wa awali walivyojiandaa kwa ajili ya kumwagiwa kwa Roho Mtakatifu Siku ya Pentekoste. Kazi hiyo hiyo, lakini kwa kiwango kikubwa zaidi, lazima ifanyike sasa .

----------------------------

Maswali: Kwa nini ahadi au nadhiri tunazozitoa kwa Mungu wetu ni muhimu? Petro alijuaje uongo wa Anania na Safira? Kwa nini Hofu ililipata kanisa lote? Kwa nini watu walitoa wagonjwa na matandiko nje? Je unataka kuwa Barnaba mwana wa matumaini au Anania na Safira wana wa kukatisha tamaa? Kufa kwa Anania na Safiri unafikiri kulileta jambo gani miongoni mwa watu? Safira alikuwa mjane kwa masaa mangapi?

**SIKU YA 299.**
**(Oktoba 25)**

# Mitume wawekwa gerezani mara mbili.

**Matendo 5.**

Kuhani mkuu na makuhani wenzake walikuwa masadukayo, na wakaingiwa na wivu, maana hawakuamini ufufuo, wala Malaika. Hawa waliwakamata mitume na kuwaweka ndani ya gereza. Lakini Malaika alifungua milango ya gereza usiku akawatoa, na kuwaambia "Enendeni mkasimame hekaluni mkawambie watu Maneno yote ya uzima ya Injili. Wakaenda hekaluni alfajiri na kuanza kufundisha. Kuhani mkuu na watu wa baraza la Sanhedrini walikutana kujadili wawafanyie nini mitume. Walipoenda gerezani walikuta hamna mtu, na walinzi wako nje wakiendelea kulinda wasijue. Wazee wote wa Israeli kwa kawaida walikuwa 71.

Mambo ya Mafarisayo na Masadukayo, yameandikwa kama mfano kutusaidia sisi tunaoishi mwisho wa wakati! Tunapojitolea kufanya kazi ya Bwana kwa kutii maagizo ambayo tumepokea kupitia Neno Lake, Yeye atatutumia kumaliza kazi Yake, hata kama hali zinaonekana kukosa matumaini. Zaidi ya hayo, Atabadilisha mioyo yetu pia, na kutufanya kuwa wasafi, watakatifu na wenye furaha katika huduma Yake. Hatutakuwa watenda kazi wa mshahara au walei wenye siasa. Hebu tuamke, na kujinasua kutoka mikononi mwa adui, na kuvaa silaha, ili tuweze kupigana kwa bidii na adui mjanja, ambaye anatembea kama simba angurumaye kutafuta mawimdo ili ammeze muumini. Yeye hangurumi kila wakati, huwa anapotimiza kusudi lake vyema zaidi, huzamisha sauti yake chini na kunong'ona kwa upole zaidi, na, akiwa amevikwa mavazi ya nuru, anatokezea kama malaika kutoka mbinguni. Wanadamu wana ujuzi mdogo sana wa hila zake, na siri zake zenye uovu. Ni Bwana tu Ndiye awezaye kutusaidia kwenye mapigano. Wale wanaopenda porojo, na umbeya wa kusema makosa ya huyu na yule, waamke pia, na kujiangaila ndani ya mioyo yao wenyewe. Wasome Biblia, na kwenda kwa Mungu katika sala ya bidii. Tumwombe atufundishe kuujua moyo wetu wenyewe, kuelewa madhaifu yetu, dhambi zetu na upumbavu wetu katika ile nuru ya milele. Tumwambie Mungu atuonyeshe tunaposimama sisi wenyewe mbele za mbingu. Haya ndiyo maombi tunayopaswa kutoa tunapokutana na upinzani kama ule wa kanisa la awali.

Basi wakuu wa makuhani na Jemedari wa hekalu wakiingiwa shaka kwamba mambo yatakuwaje wasijue kwamba mitume wako huru na wanaendelea kupeleka Habari njema, mtu mmoja alikuja kuwapasha habari "watu wale mliowaweka gerezani wamesimama kwenye hekalu wakifundisha watu!" Kuhani mkuu alimwambia Jemedari yaani askari wa hekalu awakamate ila kwa kutumia hekima maana walihofu fujo zisije zikatokea na watu watawapiga mawe, maana wengi walikuwa wamegundua hila za makuhani, na hata kumwamini Yesu, Masihi.

Wakaitwa barazani na kuhani mkuu, naye akawauliza "Je hatukuwaamuru ninyi kwa nguvu, msifundishe kwa jina hili? Nanyi mmejaza mafundisho yenu Yerusalemu,

mkitaka watu waamini kwamba tuna hatia ya kumwua Yesu." Petro alisema kwa ujasiri "imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu." Akaeleza Mungu wa Baba zetu alimfufua Yesu ambaye ninyi mlimwua na kwa kumtundika msalabani. Mungu amemtukuza Yesu, kwa mkono Wake wa kuume awe mkuu na Mwokozi, awape Israeli Toba na msamaha wa dhambi, na sisi tu mashahidi wa hayo na Roho Mtakatifu Ambaye ametolewa kwa kila mtu anayetii. Waliposikia hayo walichomwa moyo kwa hofu. Dhamira zilipowashitaki badala ya kutii na kumwamini Yesu walitaka kuwaua ili wasiendelee 'kuwabugudhi'.

Ila Mfarisayo mashuhuri aitwaye Gamalieli ambaye ni mtu wa baraza, na mwalimu wa torati ajulikanaye sana, na kuheshimiwa na watu, Alisimama barazani na kusema "Enyi wanaume wa Israeli jihadharini mtakavyowatenda hawa watu." Akawapa mifano ya Theuda zamani kidogo, aliyejidai ni mtu mkuu. Huyu alisema ni mkombozi, na akawa na watu 400 walio tayari kupigana na kuiweka Israeli huru, lakini aliuwawa na wafuasi wake. Wale waliomsadiki, walitawanyika, wakawa si kitu. Kisha akaja Yuda Mgalilaya. Siku za kuchukua Sensa, wakati Yesu alizaliwa na kuvuta watu kadhaa wamfuate aliongoza upinzani mkubwa Naye pia akapotea na watu Wake wakatawanyika. "Basi nawaambieni jiepusheni na watu hawa, waacheni, kwa kuwa kama shauri lao ni kazi ya binadamu litavunjwa, lakini kama limetoka kwa Mungu, hamwezi kuivunja kazi Yake. Jihadharini msije mkaonekana kuwa mnapingana na Mungu." Wakakubali Maneno ya Gamalieli aliyepewa hekima ya Roho wa Mungu kwani alikuwa mcha Mungu.

Wakawaita mitume na kuwatandika viboko kisha wakawamuru wasinene Jina Lake Yesu. Kisha waliwaweka huru waende zao. Viboko viliuma ila mitume walitoka na furaha katika ile baraza, kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina Hilo. Wakaendelea kila siku kufundisha habari njema za Yesu Kristo ndani ya nyumba zao na hekaluni. Hakika tumepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu Yeye, ila na kuteswa kwa ajili yake. Tunaambiwa kuwa tuhesabu kuwa ni furaha tupu kila tunapopatwa na majaribu ya namna nyingi, kwa maana tunajua kwamba kujaribiwa kwa imani yetu huleta saburi. Tuache saburi imalize kazi yake, ili tupate kuwa wakomavu na watimilifu, bila kupungukiwa na kitu.

Yesu anakuja hivi karibuni. Tushike sana tulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yetu. Mateso ni jambo la huzuni. Mara nyingi husababishwa na hasira, chuki, wivu na ghadhabu. Nchi nyingi leo hasa zile za Asia na Afrika ya magharibi zina utesi mwingi kwa waumini. Mfano Korea ya kaskazini, na Somalia. Ukiona unateswa, basi mwombe Mungu akupe nguvu na hekima ya kukusaidia kufanya jambo lililo sawa. Shauriana na waumini wenye hekima. Mungu ametukumbusha mara kwa mara kupitia injili yake kuomba bila kukoma. Biblia ina maelfu ya mistari inayohusu ahadi za jinsi ya kuchukuliana na mateso. Jitolee kusoma Maandiko kila siku kwa sababu majibu ya Mungu daima yanapatikana katika Biblia na Maombi. Tutakumbuka kwamba tunapaswa kumtumaini Mungu kwenye mioyo yetu wakati wa huzuni na kutokata tamaa na pia kuwasamehe na hata kuwaombea maadui zetu. Mateso na maumivu yetu hapa duniani ni ya muda. Kwa hivyo kuwa na subira na kuendelea kukiri imani yetu kwa bidii na kumshukuru Bwana ni muhimu, kwa kuwa thawabu zetu za milele zinatungojea katika ufalme wa Mungu huko mbinguni!

Tudumu katika imani na kuombeana.

* Nyumba za Wakristo zinapaswa kuwa taa ulimwenguni. Kutoka kwao, asubuhi na jioni, sala inapaswa kupanda juu kwa MUNGU kama uvumba unaonukia. Na kama umande wa asubuhi, rehema Zake na baraka zitashuka juu ya waombaji.


--------------------------------

Maswali: Kwa nini mitume waliwekwa gerezani? Gamalieli alitoa ushauri gani? Kwa nini imetupasa kumtii Mungu kuliko mwanadamu? Sanhedrini ni nini? Kwa nini makuhani hawakupenda kusikia kwamba wao ndiyo walimwua Kristo? Tufanyeje wakati wa mateso?

**SIKU YA 300.**
**(Oktoba 26)**

# Stefano auwawa.

**Matendo 6.**



Siku zile watu waumini walizidi kuongezeka na kukahitajika utawala au urasimu wa kupanga mikakati. Kukua kwa shirika lolote kunahitaji mifumo na uongozi. Kukawa na manung'uniko au kutoelewana kwani Wayunani (Wagiriki) na wahamiaji walikuwa na wajane wao waliosahahuliwa katika huduma ya kila siku. Pengine ilikuwa ni kubaguliwa, au kutumia lugha tofauti kwa hawa Wayunani, waliojiunga kama Wakristo wapya kulikofanya mawasiliano yaharibike. Watu walikuwa wameaminiana mwanzo, sasa wakaanza kushukiana. Mahitaji yao ya muhimu kama chakula, kusaidiwa wakiwa wagonjwa, na huduma nyingine yakasahauliwa.
Mitume wakawaita waumini na kuwaambia "haipendezi sisi kuacha kuhubiri Neno la Mungu na kugawa chakula, kuwa watunza hazina au kushughulika kuamua magomvi. Basi ndugu chagueni watu saba miongoni mwenu walioshuhudiwa vyema wenye kujawa na Roho na hekima ili tuwaweke kuwa viongozi wa huduma hiyo, ili nasi tupate muda kwa kuomba, kujiweka wakfu na kuhubiri Neno. Kazi ya kwanza ya kanisa ni kutangaza wokovu kwa kila mtu. Hii yapaswa iwe shughuli ya kwanza kwa kila binadamu. Kusafisha, kupika, kulima, kwenda kibaruani, kusanya kuni, kuwasha moto kwapaswa kuja baada ya kuhubiri injili. Kazi ya pili ya kanisa ni kushughulikia wenye mahitaji, masikini, wajane, yatima, masikini wageni na wagonjwa, walio magerezani, na kutunza mazingira ya kanisa. Kazi ya ushemasi ni kazi ya utawala au uongozi ili kusaidia injili kwenda mbele.

Neno hili likawapendeza mkutano wote, na wakamchagua Stefano, aliyejaa imani na Roho Mtakatifu na Filipo, Prokro, Nikanori, Timoni, Parmena, na Nikolao wa Antiokia. Wakawaweka hawa mbele ya mitume ambao waliwaombea na kuwawekea mikono kwa huduma hii maalumu kama alama ya baraka za Mungu juu yao. Wengi toka siku zile wameendelea kuwawekea mikono watumishi kwa huduma ya kazi ya

Mungu. Neno la Mungu likaendelea kuenea sana, hata wakuu wa makuhani wengi wakampokea pia. Hii inatia moyo, maana Yesu alifanya kazi asione matunda haya. Alikuwa amepanda mbegu na wanafunzi Wake walikuja kuvuna.

Kile kifo Chake na kufufuka Kwake, vilikuwa mahubiri makubwa na sumaku ya kuwavuta watu Kwake, kama alivyosema "Nikiinuliwa nitawavuta watu wote Kwangu." Unabii wa Yesu mwingine, kuhusu kazi ya mitume kuhubiri, ulitimia kwa kupitia uwezo wa Roho wa Mungu, kwamba wangefanya mambo makubwa zaidi. Stefano hakufanya huduma ya ushemashi tu, bali akiongozwa na Roho Mtakatifu alihubiri na kupewa neema ya kutenda miujiza na ishara kubwa katika watu. Ila baadhi ya watu wa Sinagogi Huru waliotoka Kirene Libya, na Iskanderia Misri, na Kilikia na Asia waliondoka kubishana na Stefano, ila Roho Mtakatifu alimpa Stefano hekima na aliwajibu kwa hekima ya Roho wasiweze kumshinda.

Wakamtungia maneno kwa watu "tumemsikia akinena maneno ya kumtukana Mungu na Musa." Wakafanikiwa kuwashawishi wazee na waandishi wa Sheria ya Musa kumwendea, na kumkamata Stefano na kuletwa kwenye Baraza kuu la Wayahudi la Sanhedrini. Wakala rushwa kwa kuweka mashahidi wa uongo waliosema "Stefano haachi kusema maneno ya makufuru, tumemsikia akisema Yesu Mnazareti atarudi na kupaharibu mahali hapa na kuzibadili destruri tulizopewa na Musa." Hapo ndipo wazee wa baraza hilo walimkodolea macho ya uovu, na wakamwona uso wake uking'aa kama wa Malaika, kwa ile imani aliyokuwa nayo.

Kuhani akamwuliza, kama watu wasemayo ni Kweli? Stefano aliomba watu wamsikilize akitoa historia ya Israeli, anapojitetea. Akaanza na historia ya Ibrahimu miaka ya 2091 Kabla ya Kristo, aliyeitwa na Mungu kutoka nchi yake ya Ur kule Mesopotamia, ambayo ni Ukaldayo au Iraki  ya leo, na kwenda Kanani. Mungu akasema wazao wake watakuwa wageni kwa miaka zaidi ya 400, kisha atawatoa utumwa wamwabudu Kanani ambapo ni Israeli miaka ya 1446 KK. Akampa Agano la Tohara. Akazungumza ya Isaka miaka ya 2066 KK, Yakobo miaka ya 2006KK, Yusufu miaka ya 1885 KK, na hata Musa toka utoto 1570 KK mpaka alipovua viatu vyake alipoambiwa na Mungu. "BWANA Yule aliyewatoa akifanya ajabu na ishara katika nchi ya Misri."

Musa aliwaambia Waisraeli Mungu atawainulia nabii kati ya ndugu yenu. Yeye ndiye aliyekuwa kanisa la Jangwani, na mlima wa Sinai mwaka 1450KK, na ndiye aliyepokea Maneno ya uzima atupe sisi, ila Wanaisraeli baba zetu walimsukuma mbali. Akasema "Enyi wenye shingo ngumu, siku zote mnampinga Roho Mtakatifu kama baba zenu, ni nani katika manabii baba zenu hawakumwudhi? Waliua wale waliotabiri habari za kuja Kwake Mwenye Haki Yesu, Ambaye ninyi mlimsaliti na kumwua, ninyi mlioipokea Sheria ya Sinai msiishike."

Wale wakuu wa baraza waliposikia haya walipata hasira, mioyo yao ikawachomwa, kiburi chao kilishushwa wakasaga meno kwa jazba. Naye Stefano alikaza macho yake mbinguni, naye akijaa Roho Mtakatifu akaonyeshwa maono ya utukufu wa Mungu na Yesu akisimama upande wa kuume wa Mungu. Akasema "Tazama! Naona mbingu zimefunguka na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume

wa Mungu." Wakapiga kelele na kuziba masikio na kumrukia, wasiwe waungwana mahakamani; kwani hata mahakamani jaji hawezi kufunga masikio yake asimsikilize mtuhumiwa akiwa mbele za watu kabla ya hukumu kutolewa. Basi wakamtoa nje ya mji wampige mawe, ili wasinajisi hekalu. Walijali hekalu lao zuri kuliko Mungu au manabii Wake.

Hekalu ni muhimu, ila Yule anayelifanya kuwa takatifu ni Mungu. Pia ni muhimu kuweka mioyo yetu sawa. Hawakujua kwamba mioyo yetu ndiyo hekalu la kwanza, kabla ya majengo ya kazi za mikono ya mwanadamu. Walijaa mafundisho mengi yasiyowasaidia kwenye ubongo, mioyo yao ilijaa dhambi, chuki na wivu. Mashahidi wakaweka nguo zao miguuni pa kijana aitwaye Sauli, nao wakampiga Stefano kwa mawe. Naye akikata roho alilia kwa sauti kuu "BWANA Yesu pokea roho yangu, BWANA usiwahesabie dhambi hii" ndipo akafa. Sauli aliona hili ni jema, naye aliwekwa kuwa mmojawapo wa baraza la wazee wa Sanhedrin. Kutoka siku hiyo akaongoza ukatili kwa kanisa changa lililoanza Yerusalemu.

Twapaswa kushukuru uhuru wa kuabudu tulio nao sasa, maana siku hizi mtu akipelekwa mahakamani kwa kosa fulani, mahakimu hawafungi masikio na kumpiga mawe. Adhabu hutolewa baada ya kutumia muda kufanya upelelezi. Twapaswa tuwe watu wenye uvumilivu hata kama mtu ana imani tofauti na yetu. Jambo hili linaitwa uhuru wa dini au uhuru wa kuabudu. Hata pale ambapo watu hawamwabudu Mungu wa mbinguni twapaswa kwenda kushaurina nao kwa upendo kwamba kile wanachokifanya si chema au ni dhambi, ila hatupaswi kuwaua. Maana Mungu hajatuambia tufanye hivyo, serikali iliyotawala Israeli wakati wa Agano la Kale ilikuwa inaongozwa na Mungu (theocracy) hii iliendesha mambo kutokana na maagizo ya Mungu, kwani Mungu ni mhukumu pekee mwenye haki, na upendo wote. Yeye peke Yake Ndiye Mwenye rehema yote, upendo wote na haki yote na anajua jinsi ya kuvioanisha au kuvibainisha hivyo vitatu.

Hata kwenye jeshi ni vyema tukahusika kwenye kusaidia majeruhi zaidi ya kuua adui au watu ambao tumegombana nao. Kuna kazi nyingi za kufanya jeshini ambazo hazihitaji kushika bunduki kwenda kuua watu. Waumini wengi hufurahia majeshi ya nchi zao yanapowashinda raia wa nchi nyingine kwenye vita, na wanasimulia kwa uhodari wale waliouwawa bila ya kuchuja kwamba maisha ya mtu yana thamani gani kwa Mungu. Wakati mwingine hili lawezekana kuwa ndilo la kufaa kufanya, kama Tanzania ilipoenda vitani na Uganda, ila vita nyingi ni magomvi madogo madogo au chuki na hasira za watu wa ngazi za juu. Mfano mzuri ni vile vita vikuu vya kwanza vilivyotokea kutokana na mauaji ya Archduke Franz Ferdinand wa Austria-Hungary mnamo Juni 1914 na kikundi cha Black Hand. Jambo hili lilianzisha vita na lilisababisha watu milioni 40 kufa! Hata babu ya mama yangu aliyeitwa Makori kutoka Mara Tanzania alichukuliwa na wenzake na jeshi la Uingereza kwenda India mwaka 1919 kupigana vita hivi. Unaweza kushangaa kama mimi, kwamba India ilihusikaje basi na mtu aliyeuwawa Austria, na Tanzania Je, ilihusikaje! Pengine hiki ndicho kilikuwa chanzo cha kuanzishwa kwa jumuiya ya nchi zisizofungamana na upande wowote.

Madhehebu mengi yamepata shida kwa hapa nchini Marekani katika jinsi ya kutimiza wajibu wao kama raia wema wa nchi, na pia waumini wenye hofu ya Mungu. Wanaona si vyema katika dhamira zao  kubeba silaha au kulazimishwa kubeba silaha ili kuua watu ambao wanajua fika nchi yao inafanya makosa kuwachokoza au kuwaonea  eti ni kwasababu ya nguvu zao. Wao wenyewe husema "sisi ndiyo mbwa mkubwa kwenye mtaa wa dunia!" (We are the big dog on the block). Baada ya maombi mengi na utafiti wa kina viongozi wa makanisa kadhaa walihitimisha kwamba nafasi nzuri ya kuchukua ilikuwa kanuni ya kutopigana (non-combatant). Msimamo huu ukasajiliwa rasmi kwenye serikali  ya Marekani mwaka wa 1864 na umesalia kuwa msimamo wa madhehebu kadhaa. Hakika tunahitaji hekima hata na wenzetu mashuleni, ukiona watu wanampiga mtoto fulani, je, nawe utajiunga kumpiga wakati unaona kwamba anaonewa na vijana ambao ni wababe au waonevu (bullies)?

*Upendo kwa roho zinazoangamia ulimsukuma/ulimbidisha Ibrahamu kusihi. Wakati alikuwa anachukia dhambi za mji huo wenye ufisadi, matamanio yake yalikuwa kwamba wenye dhambi waweze kukolewa. Kuijali kwake Sodoma kwa kina kunaonyesha wasiwasi ambao tunapaswa kuhisi kwa wale wasiotubia dhambi zao. Tunapaswa kuichukia  dhambi mioyoni mwetu, lakini kumwonea huruma  na na kumpenda mwenye dhambi.

-----------------------------

Maswali: Kwa nini mashemashi wanahitajika kwenye kanisa leo? Taja majina saba ya mashemasi wa kwanza. Sifa za Stefano zilikuwa zipi? Stefano alipataje nafasi ya kushuhudia watu kuhusu Kristo?  Kwa nini watu walimwua Stefano? Kazi ya kwanza ya kanisa ni nini? Kwa nini Stefano hakuwa na hasira bali aliwaombea waliomwua? Kutokana Maandiko kwamba miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu, waliomwua Stefano walikuwa wamelinajisi hekalu tayari kwa namna gani?

**SIKU YA 301**
**(Oktoba 27)**

# Sauli atesa watakatifu na kanisa.

**Matendo 8.**




Kwa ajili ya utesaji Wakristo, waumini walianza kutawanyika katika nchi ya Uyahudi, Misri, Kupro Italia, Hispania, Kaisaria na Samaria. Ila Mitume waliendelea kukaa Yerusalemu. Watu wakamzika Stefano, kwa maombolezo makuu. Mambo yote yalikuwa yameendelea vyema, Wakristo hawa wapya walijiuliza, mpaka kuuwa kwa Stefano. Waumini walipata shida nyingi, ila Mungu alifanya miujiza mingi pia ya kuwalinda. Wakuu wa makuhani hawakutaka dini hii changa ambayo Kristo alileta, baada ya kuona mfumo wa zamani haukusaidia watu. Ili kupiga vita Ukristo usienee, walitafuta njia za kutesa waumini hawa.

Mtu mmoja wa baraza la Wayahudi aitwaye Sauli akaingia majumbani mwa watu na kuwaburuza waumini, wake kwa waume na kuwatupa gerezani, akidhania anamfanyia Mungu kazi. Siku zile watoto wa waumini walipata shida kwani wazazi wao waliwekwa magerezani na kuteswa; Ila wengi waliotoka kwenda miji mingine waliendelea kupeleka habari njema za Yesu Kristo. Wayahudi walifanya makosa kudhani kuwa kwa kuwa wamemwua Yesu basi na injili haitafanikiwa. Kwani kadri walivyozidi kuwaua ndivyo ilikuwa mbegu ya kuwafanya wengi waamini na wawe mashujaa zaidi. Katika mateso yoyote ya dini jambo hili hutokea, tuliona kule nchini Uganda na Rwanda, baada ya mateso, watu wengi walipata uamsho na matengenezo na kushika kazi ya Mungu kwa matamanio makubwa.

Filipo aliyeanza kuhudumu kama shemashi, alitoka akaenda Samaria akimhubiri Kristo. Watu walikuwa na shauku ya kumsikiliza, na miujiza ikatendeka kupitia yeye. Pepo wachafu wakatoka watu wengi waliopagawa, nao wakalia kwa sauti kuu. Viwete, na vipofu wakaponywa na furaha kuu ikaingia katika mji ule wa Samaria. Wale waliomfukuza Yesu asiingie kijijini kwao na kuwabariki, walikuwa tayari kupokea Neno la Yesu sasa. Hakika nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.

Mtu aitwaye Simoni mchawi, pale mjini Samaria alikuwa akipata pesa kwa miujiza aliyokuwa akiifanya na akadai yeye ni mtu mkubwa. Watu walimsikiliza, watoto kwa wakubwa. Ila Filipo alipokuja akihubiri habari njema za Ufalme wa Mungu na Jina Lake Yesu Kristo, watu wakamwamini na kubatizwa wanaume kwa wanawake. Ubatizo huu twasimuliwa kuwa ndiyo ulikuwa wa kwanza nje ya nchi ya Uyahudi. Hata huyu mchawi akadai ameamini na akabatizwa na alipoona ishara na miujiza alistaajabu akitaka naye apate uwezo huo, maana alijua uwezo wake wa kichawi ulikuwa hafifu kulinganisha na ule wa Filipo.

Tujue kwamba Shetani, hana uwezo unaowezwa kulinganishwa na uwezo wa Mungu kwa kuwa yeye ni kiumbe tu. Mitume waliposikia Samaria imepokea Neno la Mungu, waliwatuma Petro na Yohana nao walipofika waliwaombea wapokee Roho Mtakatifu kwa maana walibatizwa kwa Jina la Yesu ila walikuwa hawajapokea Roho Mtakatifu. Petro na Yohana wakaweka mikono yao kwa waumini waliobatizwa nao wakapokea Roho Mtakatifu na Simoni alipoona ya kuwa wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono na mitume, akataka kuwapa pesa mitume ili wampe naye uwezo huo. Simoni alitaka "kila mtu atakayemwekea mikono yake apokee Roho Mtakatifu." Maskini hata haukujua Roho Mtakatifu ni nani.

Petro akamwambia, fedha yako ipotelee mbali pamoja nawe, kwani umedhania kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali "Huna fungu wala huna sehemu katika huduma hii kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele ya Mungu basi tubia uovu wako huu ukamwombe BWANA ili usamehewe mawazo haya maovu. Ilibidi atubu kwa maana aliona wivu kwa karama Mungu aliyoitoa kwa mitume. Hata hivyo Mungu hapokei rushwa, kwamba tumpe pesa ndiyo atupe sisi wanadamu Roho Mtakatifu. Simoni akajibu "niombeeni ninyi katika BWANA yasinifike mambo haya, hata moja." Mitume na Filipo wakaendelea kuhubiri injili katika vijiji vingi vya Samaria

*Bwana akasema, "Nitafanya jambo hili pia ulilolinena; kwa kuwa umepata neema mbele Zangu, na nakujua kwa jina." Bado nabii huyo Musa, hakuacha kuomba kwa kusihi. Kila sala ilikuwa imejibiwa, lakini alikuwa na kiu ya ishara kubwa za upendeleo wa MUNGU. Sasa alifanya ombi ambalo hakuna mwanadamu aliyewahi kufanya hapo awali: "Ninakuomba, nionyeshe utukufu Wako."
---------------------------

Maswali: Kwa nini waumini wa kwanza walitawayika? Kwa nini ilikuwa mbaraka kwa jinsi fulani kwa waumini kutawanyika? Filipo alifanya kazi gani kijiji cha Samaria? Kwa nini Petro alimkaripia Simoni? Kwa nini kuona wivu wa karama za wengine ni dhambi? Kwanini Roho Mtakatifu hawezi kununuliwa?

**SIKU YA 302.**
**(Oktoba 28)**

# Filipo na towashi wa Ethiopia (Kushi).

**Matendo 8. Isaya 53.**



Wakati Filipo anaendelea na kazi Samaria, Malaika wa BWANA akamwambia Filipo kwenda kusini njia itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza nayo ni jangwa. Bila kuuliza na kubishana akatii. Akiwa njiani kwenda kule mara akamwona mtu wa Kushi au Ethiopia aliyekuwa amesafiri zaidi ya km 1500 kuja kuhiji na kuabudu Yerusalemu. Huyu alikuwa towashi mwenye mamlaka ya waziri wa hazina, katika himaya ya Kandake malkia wa Ethiopia. Watu hawa wa Ethiopia walikuwa wamemjua Mungu wa mbinguni na Agano la Kale kwa miaka mingi.

Mhabeshi au Mkushi huyu alikuwa anarudi nchini mwake, ameketi kwenye gari zuri la fahari akisoma chuo cha nabii Isaya. Roho akamwambia Filipo sogea karibu naye, naye Filipo akaenda kwa mbio, akamsikia anasoma kwa sauti kile kitabu cha nabii Isaya. Akamwuliza yule Mkushi "Je yanakuelea haya unayosoma?" naye akajibu "Nitawezaje kuelewa Maandiko haya ya Wayahudi mtu asiponiongoza?' Ndipo akasimamisha gari la farasi, na kumwambia Filipo akae pamoja naye kwenye gari, na sura aliyokuwa akisoma yule towashi Mkushi ni Isaya 53. Sura hii

hii imezungumza kuhusu mateso ya Yesu, na kafara aliyotoa kama Mwanakondoo wa Mungu ili achukue dhambi zetu. "Aliongozwa kwenda machinjioni kama kondoo alivyo kimya mbele yake amkatae manyoya…" Tafadhali endelea kusoma Sura hii Kwenye Biblia!

Towashi akauliza yamhusu nani Maneno haya?" Akasubiri kwa shauku kuelezwa maana alikuwa mtu anayempenda Mungu ila hakujua habari za Masihi Yesu aliyezaliwa, na Aliyekufa kwa ajili yetu na kupaa mbinguni. Filipo alifananua Maandiko yale kwamba yalimhubiri Yesu. Akamweleza unabii wote wa Agano la Kale na jinsi ulivyotimia, na hata kufa na kufufuka kwa Yesu, na jinsi atakavyorudi tena. Akamweleza hatua za kuwa muumini wa Yesu, ikiwa na maana ya ubatizo kama vile Nikodemu alivyoelezwa kuhusu kuzaliwa kwa maji na kwa Roho. Yalikuwa masomo au Mafundisho ya Biblia mazuri. Filipo na Mkushi wakaona ni Mungu amewaongoza wakutane.

Gari likiwa linaendelea kwenda tu, basi wakafika mahali penye maji, na yule towashi akasema "Tazama, maji ni haya, nini kinazuia nisibatizwe hapa saa hii?" Filipo akamwambia, "Ukiamini kwa moyo wako wote, Yesu ni BWANA na Mwokozi wako inawezekana." Towashi akajibu "naamini Yesu Kristo Ndiye Mwana wa Mungu na Mwokozi wangu." Towashi alikuwa amempenda Yesu na kutaka kumfuata njia yote, Filipo Akamwambia dereva wa gari asimame pale, wakatelemka wote majini, Filipo akambatiza yule towashi. Walipotoka ndani ya maji, Roho wa Mungu alimnyakua Filipo akaonekana tena Azoto, na huko aliendelea kuhubiri Injili katika miji yote hata akafika Kaisaria. Naye Mkushi akaenda akiwa na furaha moyoni mwake kama mmishionari Mwaafrika aende kuwaambia watu habari njema. Huyu Filipo ndiye aliyekuwa na binti wanne wenye Karama ya Roho ya kutabiri. Hata leo hivi wengine hubatizwa baada ya kusoma Maandiko majumbani mwao, ila wanahitaji kusaidiwa mahali pachache wanapopata utata katika Maandiko. Ni vyema mtu afundishwe vyema Maandiko kabla ya kubatizwa, na mara nyingi hupewa maswali kuona kama hayo aliyofundishwa ameyaelewa.

Masomo yanayofundishwa ni kama Kwanini Biblia ni Neno la Mungu linalopaswa kuaminiwa? Yesu, Mungu na Roho Mtakatifu ni nani? Jinsi ya kuielewa Biblia, Hukumu ya siku ya mwisho, Unabii wa Danieli 2, Jinsi Yesu atakavyokuja, unabii mrefu wa Biblia, Upendo wa Mungu na moto wa Jehanamu, dhambi isiyosameheka, kuwa na amani moyoni, mtindo wa maisha wenye afya, kuwa na mafanikio kiuchumi n.k

Sauli alizidisha chuki kwa kutesa na kutisha watakatifu, hata kuwazia, na kuwaua wanafunzi wa BWANA. Siku moja akamwendea kuhani mkuu ampe barua ya ruhusa aende hata Dameskiki, kwenye masinagogi kutafuta Wakristo. Aliomba barua yenye mamlaka ili aipeleke kwa wakuu wa masinagogi wawatoe Wayahudi wote wanaomwamini Yesu. Sauli Mfarisayo, akawa adui mkubwa wa Wakristo, na kila mtu akamwogopa.

*Bwana aliahidi kuwaepusha Israeli na uharibifu wa haraka; lakini kwa sababu ya kutokuamini kwao na woga hakuweza kudhihirisha nguvu Zake katika kuwashinda adui zao. Kwa hiyo kwa rehema Yake aliwaamuru, kama njia pekee salama, warudi nyuma kuelekea Bahari ya Shamu.
------------------------------

Maswali: Je mtu aweza kuwa shemasi na Mwinjilisti? Filipo alikutanaje na towashi? Mkushi alimwambia nini Filipo walipokutana? Kwa nini Mkushi alienda kwao akifurahi? Sauli alienda Dameski, Syria kufanya nini? Injili ni nini?

**SIKU YA 303.**
**(Oktoba 29)**

# Sauli atokewa na Yesu.

**Matendo 9.**



Kijana Sauli alikuwa Mfarisayo mwenye imani ya ushabiki ya ya kupitiliza na chuki (fanatic), alienda kaskazini, Dameski huko Syria, kilomita 200 hivi, kuwafuata watakatifu katika nchi hiyo awarudishe Yerusalemu ili awatese na kuwamaliza kabisa. Akiwa kwenye msafara kwa siku kadhaa, maana ilichukua siku kadhaa kufika, akikaribia mji na wenzake, kwa ghafla nuru kali kama ya radi, ikamwangaza kote kote kutoka mbinguni naye na wenzake wakasimama. Sauli Akaanguka chini, akasikia sauti ikizungumza naye "Sauli, Sauli mbona Wanitesa." Sauli kwa kuchanganyikiwa alijibu "U nani Wewe BWANA?" Sauti ilimjibu "Mimi ni Yesu unayeniudhi wewe, lakini nenda mjini nawe utaambiwa yakupasayo kutenda."

Na wale waliosafiri pamoja naye, walisimama kimya wakiisikia sauti, wasione mtu. Sauli aliinuka toka chini, na macho yake yalipofumbuka, hakuona kitu, alikuwa kipofu. Akijikwaa hapa na pale kwa kuongozwa, asiweze kufika Dameski kwa vishindo na vitisho alivyopanga. Akapata muda wa kunyenyekea na kujutia maovu aliyoyafanya, naye akawa chombo kiteule. Ule mori na nguvu za kufanya maovu, ukageuka kuwa mori wa kumfanyia kazi Yesu. Huyu ni mfano kwetu sote tunavyopasa kuwa. Wakamshika mkono wenzake na kumpeleka Damesiki na akakaa huko siku tatu, bila kunywa, wala kula akitafakari kuhusu Yesu, Ambaye alijua sasa wazi kwamba anamwuudhi.

Pengine alikuwa na nafasi ya kurudi nyuma na kuangalia unabii wa Masihi akagundua kwamba Yesu ni Masihi wa Kweli, Yule aliyeahidiwa. Kabla ya hapo alikuwa amefanya uovu akifikiria yuko sawa na anamfanyia Mungu kazi njema. Wayahudi walitaka kujua nini kimetokea na Wakristo walitaka kusikia ushuhuda wake. Kule Damesiki kulikuwa na mwanafunzi wa Yesu Kristo aitwaye Anania. BWANA akamwamwita katika maono "Anania" naye akasema "Mimi Hapa BWANA." Naye akamwambia "Simama uende njia iitwayo nyofu, ukaulize katika nyumba ya Yuda mtu aitwaye Sauli wa Tarso, anaomba na kufunga sasa akiulizia msaada. Nami nimemwonyesha kwa njia ya maombi kwamba mwanafunzi aitwaye Anania, atakapoingia atamwekea mikono juu yake, ili apate kuona tena."
Lakini Anania kwa woga akijua hakuna muumini aliyetaka kumsogelea mkatili Sauli, alijibu "BWANA nimesikia habari za mtu huyu kwa watu wengi, mabaya mengi aliyowatenda watakatifu wako Yerusalemu akiwakamata na kuwaweka magerezani." Anania akasema amesikia pia kwamba Kuhani mkuu alimpa mamlaka ya kuwakamata watu Dameski na kuwarudisha Yerusalemu. BWANA akamwambia "nenda tu maana ni chombo kiteule Kwangu, alichukue Jina Langu mbele ya mataifa, wafalme na wana wa Israeli, maana nitamwonyesha yaliyo mengi yatayompasa kuteswa kwa ajili ya jina Langu."

Anania akaenda na kuingia mle nyumbani, kisha akaweka mikono yake kwa ndugu Sauli akisema "Ndugu Sauli, BWANA amenituma, Yeye aliyekutokea njiani ukija hapa Dameski, upate kuona tena na ukajazwe na Roho Mtakatifu." Mara vikaanguka vitu kama magamba, akapata kuona, akasimama na akabatizwa, akala chakula na kupata nguvu. Kuanzia pale wale waliomjua walimwita Paulo kwa jina lake la Kirumi, maana yake ni mdogo au mnyenyekevu. Akakaa siku kadhaa na wananafuzi walioko Dameski, akimhubiri Yesu katika masinagogi, kwamba ni Mwana wa Mungu. Nao wote waliosikia wakashangaa wakisema "Siyo huyu aliyewatesa watu waliomwabudu Yesu na akaenda nyumba kwa nyumba kuwaburuta, hata Dameski alikuja kwa kusudi hilo, awafunge Wakristo na kuwapeleka kwa wakuu wa makuhani?"

Sauli akazidi kuwa hodari wa kuhubiri kwa nguvu na uwezo wa Roho Mtakatifu akiwaonyesha watu Maandiko kwamba Yesu ni Masihi. Wayahudi waliobishana naye hawakuweza kukataa kile alichohubiri maana kilikuwa wazi. Sauli adui akawa ndugu katika Kristo, mara alipofumbuliwa macho. Wale aliowaua kwanza baada ya upofu walikuwa ndugu zake katika Kristo. Wayahudi na makuhani wakashangaa imekuwaje amejiunga na timu ya maadui zake. Baada ya siku kadhaa Wayahudi wa Dameski walishauriana wamwue, ila hila yao ilijulikana na Sauli, nao wakamvizia mlangoni mchana na usiku.

Chuki yao ilikuwa kubwa hata BWANA akamtuma aende jangwa la Uarabuni kukaa miaka mitatu akifundishwa na BWANA. Hapo alipata muda kutafakari, kusoma Maandiko na kuomba bila ya bugudha. Kisha Paulo alirudi Dameski kuhubiri. Chuki ikaongezeka kuwa kubwa hata wanafunzi wake walimtwaa usiku na kumshusha ukutani katika kikapu. Sauli akawa mtume kwa mataifa, shujaa mkubwa, katika kazi ya kueneza injili katika kanisa hili changa. Alifanya safari ndefu za kimataifa refu nne hivi wakati ambapo hakukuwa na gari wala ndege.

Akatembea kwa miguu na mashua.

Sauli akarudi Yerusalemu akijaribu kujiunga na wanafunzi nao walikuwa wakimwogopa na kumkimbia, wasisadiki ushuhuda wake kwamba anampenda Kristo kama wao tu. Hapo ndipo Barnaba Mwana wa matumaini, aliyefanya urafiki naye na kujua yaliyomtokea akampeleka kwa mitume kwa utambulisho. Akawaeleza jinsi alivyomwona BWANA njiani na alivyozungumza naye. Aliwaeleza jinsi alivyozungumza kwa ushujaa Damesiki. Basi Mitume walimchukua kama mwenzao, wakatembea naye wakitoka na kuingia ndani ya miji. Akahubiri kwa Jina la BWANA kwa ushujaa, akinena na kuhojiana na Wayahudi na hata Wayunani, nao wakajaribu kumwua, lakini ndugu walipopata habari wakamchukua mpaka Kaisaria, wakampeleka aende Tarso kwao alikozaliwa.

Sauli akaendelea kuhubiri huko, akifanya ustadi wa kutengeneza mahema, na kufikia nchi zingine duniani. Sauli alikuwa kijana, aliyesomea vyuo vikuu bora kupita vyote vya wakati wake. Lazima alikuwa na uwezo au mali, na wadhifa kwenye jumuiya. Mungu alimchagua maana alijua alifanya mambo ya ukatili kwa ujinga akifikiri anamtumikia Mungu. Wanahistoria wengine wamesema alikuwa mbunge kwenye baraza la Sanhedrin. Paulo alipoteza wadhifa wake, bali hakujali na hata anasema kwamba anahesabu mambo yote kuwa si kitu au kama kinyesi, akilinganisha na uzuri wa kumjua Yesu.

Kanisa likapata kukua kwa furaha katika Uyahudi, Galilaya na Samaria, likajengwa, likiendelea kuongezeka katika kumcha BWANA na faraja ya Roho Mtakatifu. Petro akazungumza akitelemkia watakatifu wa Lida, akamwona mtu aitwaye Ainea amelala kitandani miaka minane na hawezi kwa mwili kupooza. Petro akamwambia "Ainea, Yesu Kristo akuponya ondoka, na utandike kitanda chako." Mara moja akaamka na watu wote wa Lida na Sharoni wakampa mioyo yao BWANA.

*Juu ya mlima wa mng'ao wa uso wa Yesu (transfiguration), Musa alikuwepo na Eliya, ambaye alikuwa ametwaliwa. Walitumwa kama wabebaji wa nuru na utukufu kutoka kwa Baba kwenda kwa Mwanawe. Na hivyo ombi la Musa, alilolitoa karne nyingi zilizopita, mwishowe lilitimizwa. Alisimama juu ya "mlima mzuri", ndani ya nchi ya urithi wa watu wake Israeli, akishuhudia kwake Yeye ambaye ahadi zote kwa Israeli zimejikita kwake. Hili ndilo lilikuwa tukio la mwisho alilofunuliwa Musa katika maono wakati bado akiwa na mwili unaokufa, katika historia ya mtu huyo aliyeheshimiwa sana na Mbingu.


---

Maswali: Kwa nini Mungu hapendezwi na dini ya unafiki, chuki au kuua wengine? Sauli alienda Dameski kufanya nini? Sauli aliongolewa kwa namna gani? Kwa nini Paulo aliwekwa kikapuni? Ainea alikuwa na shida gani? Kwa nini Paulo alienda Uarabuni miaka mitatu? Twawezaje sisi kumtesa Kristo leo? Wawezaje kuwa chombo kiteule leo? Watu waendao nchi za mbali kuhubiri waitwa nani? Kwa nini Anania alikubali kutii sauti ya Mungu? Je unaposikia sauti ya Mungu ikikuita upo tayari kuitika kama Sauli? Je, mambo ya dunia ukilinganisha na yale ya mbinguni, wewe unayahesabuje? Wafilipi 3:8

**SIKU YA 304.**
**(Oktoba 30)**

# Tabitha au Dorkasi mama mkarimu afufuliwa.

**Matendo 10.**



Karibu na Yafa kulikuwa na mwanamke mwongufu mwanafunzi wa Yesu, aitwaye Tabitha au Dorkasi yaani paa. Huyu alikuwa amejaa matendo mema na sadaka alizozitoa. Yawezekana Tabitha alikuwa mpole kama paa, na anayekimbia kwa upesi kusaidia watu wenye mahitaji akionyesha huruma na kutoa faraja kwa watu. Shughuli za kusaidia watu ni nyingi iwe ukarimu kwa wageni, kushona nguo kwa watoto yatima, kufagia nyumba ya wazee wakongwe, kuuguza mgonjwa hospitali, kutembelea walio gerezani, kuzungumza na mgane mpweke, kumwongoza kipofu barabarani, au kumfundisha kusoma mtu asiyejua kusoma. Akifanya kazi hizi, kwa roho nzuri, ucheshi na roho ya upendo.

Kanisa lilimfurahia na watu wakiwa na shida walienda kwake kumweleza mambo yao. Hatujui aliumwa nini, kama ilikuwa ni maambukizo au ni magonjwa ya presha, ila aliugua sana. Basi ugonjwa wa Tabitha ukawa mzito naye akafa, na walipoosha maiti yake wakaiweka gorofani. Siku zile na hata leo Wayahudi walikuwa na kawaida ya kuzika siku ile ile. Kwa vile Lida ilikuwa karibu na Yafa, wanafunzi

waliposikia Petro yupo pale walituma ujumbe kumsihi aje asikawie. Petro alipofika ndani tu wajane wakampeleka juu gorofani wakilia na kumwonyesha kanzu na nguo alizowashonea Dorkasi akiwa hai. Petro aliomba kwa upole wote watoke na akapiga magoti akaomba kisha akaelekea ile maiti na kusema “Tabitha nyanyuka!”

Naye akafumbua macho na alipomwona Petro aliamka akaketi. Akashangaa mtume huyu mashuhuri amefikaje hapa kwangu? Petro akampa mkono amwinue na kuwaita wale watakatifu nao waje. Akamweka mbele yao akiwa mzima, ikajulikana mji wote wa Yafa na watu wengi wakamwamini BWANA. Petro akakaa siku kadha kule Yafa kwa Simoni mtengenezaji ngozi. Tabitha naye kwa ile tabia yake ya huduma, hakukaa kivivu, bali alinyanyuka na kuendelea kuhudumia watu. Watu wakafurahi ni ajabu, kwa vile msaidizi wao ‘Bibi paa’ amefufuka ili aendelea kuhudumia wengine. Hakika kuhudumia watu ni baraka kubwa, nasi leo tumepata somo tusikae kivivu na kucheza tu siku nzima, tukingojea watu watuhudumie, hata kama tuna wafanyakazi majumbani, bali tujifunze kuwahudumia wengine, na kutumia mali zetu kuwasaidia wenye mahitaji.

Petro aliwaonea huruma wale wajane na masikini na alitaka kuwasaidia. Habari njema zilikuwa hakika katika kanisa la mwanzo. Yesu alivyowapa uwezo mitume Wake na kufanya miujiza na ishara za ajabu ni mambo halisi ambayo hata leo tunapewa uwezo huo wa kuzifanya kazi hizo za Yesu. Siku zinaenda, na tunakaribia kuja kwa Yesu, tutaona ishara nyingi zaidi maana Roho Mtakatifu atamwagwa kwa wingi.


*Hana alikuwa Mwanamke wa Maombi — Hana hakutoa lawama kwa mumewe kuhusiana na ndoa yake isiyo na busara. Huzuni ambayo hakuweza kushiriki na rafiki wa kidunia, aliipeleka kwa Baba yake wa Mbinguni, na kutafuta faraja kutoka kwa Yeye peke yake ambaye alisema, “Niite siku ya shida, Nami nitakuokoa.” Kuna nguvu kubwa katika maombi. Adui yetu mkuu anatafuta kila mara kuweka roho iliyofadhaika mbali na MUNGU. Ombi kuelekea Mbinguni la mtakatifu mnyenyekevu zaidi, hutazamwa kwa ‘kuwaka moto tumbo’ na Shetani kuliko sheria za mabaraza ya nchi au maagizo ya wafalme.
------------------------------

Maswali: Tabitha maana yake ni nini? Kwa nini watu walimpenda Tabitha? Petro aliwambiaje Tabitha? Ni huduma gani unafikiri unaweza kuanza kuifanya? Watu walipoona Tabitha amefufuka walisemaje? Kwanini tunapata furaha na kutiwa moyo tukiwafanyia watu matendo mema?

**SIKU YA 305.**
**(Oktoba 31)**

# Kornelio wa mataifa Maombi yake yalisikiwa.

**Matendo 10.**



Palikuwa na mtu wa Kaisaria Urumi, jina lake Kornelio, kiongozi wa majeshi ya kikosi kilichoitwa kiitalia. Siku hizi majeshi yetu yangemwita kapteni. Huyu hakuabudu vinyago kama Warumi bali alikuwa mtauwa na mchaji Mungu wa mbinguni, yeye na nyumba yake yote. Naye alikuwa akitoa sadaka nyingi na kumwomba Mungu daima; huyu akaona katika maono wazi wazi, kama saa tisa mchana, malaika wa Mungu akamjia na kumwita "Kornelio!", Kornelio alimtizama malaika na kuogopa, akajibu "Kuna nini BWANA?" Malaika akamwambia "Sala zako na sadaka zako kwa masikini na kazi ya Mungu zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu, hajakusahau." Hakika Mungu anatilia umakini sala na sadaka zako! Mali zetu, muda wetu na burudani tunazoshiriki zinaonyesha moyo wetu ulipo. Kama tulivyoona yule mjane wa senti mbili, alivyotiwa moyo, safari hii ilikuwa ya mwanajeshi kutiwa moyo. Wako wengi jeshini wanaomtumikia Mungu wa mbinguni, na ndiyo maana majeshi yanakuwa na huduma ya Chaplensia ya kufikia watu. Maaskari wanaolinda nchi zao wakisimamia haki, wengi wameishi fungu hili la Biblia "Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki yake" au nchi yake! (Yohana 15:13)

Malaika akaendelea kumwambia atume watu Yafa wakamwite Simoni aitwaye Petro mtume, ambaye kwa sasa ni mgeni katika nyumba ya Simoni mtengeneza ngozi, ambaye nyumba yake iko pwani, na Petro atakuambia yakupasayo kutenda. Malaika alipoondoka, Kornelio, aliita watumishi wake wawili wa nyumbani na

askari mmoja mtu mtauwa katika wale waliomhudumia daima, na kuwaeleza ile njozi, akawatuma waende Yafa. Walisafiri usiku wote ule takribani kilomita 45 na walipokuwa wanakaribia mji kwenye sasa sita hivi, Petro alikuwa amepanda darini ili asali, akaumwa na njaa sana, akataka kula.

Lakini walipokuwa wakiandaa chakula, roho yake ikazimia, akaona mbingu zimefunuka kwenye maono na chombo kikishuka kama nguo kubwa, inatelemshwa kwa pembe zake nne hata nchi; ambayo ndani yake walikuwamo aina zote za wanyama wenye miguu minne, wanyama kama pweza, kamba, panya, mbwa, nyoka, punda, kombe, mbuni, nguruwe, konokono, dubu, kangaroo, Taiga, kiboko, tembo, sungura, na wengineo. Kisha akaona wanyama wengine pia watambaao, na wale warukao kama bundi, tai, kunguru, popo, jongoo na wengineo. Akiwa na ile njaa, akasikia sauti ikimjia na kusema "Ondoka Petro, uchinje ule." Petro akijua wanyama wale si wa kula, alisema "Hasha BWANA, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi. Sauti ikamjia mara ya pili ikimwambia "vilivyotakaswa na Mungu usiviite wewe najisi." Jambo hili likatendeka mara tatu, kisha kile chombo kikachukuliwa tena mbinguni."

Petro akaona shaka ndani ya nafsi yake, maana hakujua maana ya maono yale aliyoyaona. Hapo hapo wale waliotumwa na Kornelio wakasimama mbele ya mlango ule wa Simoni mtengeneza ngozi, wakauliza kama Simon Petro mtume yumo mule ndani? Petro akiendelea kufikiri haya maono, Roho wa Mungu akamwambia "wako watu watatu chini wanakufuata basi ondoka ushuke na ufuatane nao, usiwe na tashwishi, kwa maana ni Mimi niliyewatuma." Petro akashuka toka gorofani, alipowaona wale watu alisema "Mimi ndiye mnayenitafuta. Mmekuja kwa sababu gani?" Wakasema, "Akida Kornelio, mtu mwenye haki na mchaji Mungu, aliye na sifa njema kwa taifa lote la Wayahudi, alipata maono, na Malaika Mtakatifu alimtuma tuje kwako, na twende nawe nyumbani mwake bwana wetu Kornelio, apatae kusikiliza maneno toka kwako." Petro aliwakaribisha wageni hawa.

Keshoye Petro aliondoka pamoja na wale watu na ndugu sita waliokaa katika Yafa na kufuatana nao akienda takribani Kilomita 45 hivi. Na siku ya pili waliingia Kaisaria na Kornelio alikuwa akiwangojea, hali amekusanya jamaa zake na marafiki ili wasikie habari njema. Jambo hili ni jema, kuwatakia marafiki na ndugu zetu mema waje kusikiliza habari njema za Injili ili wasipotee, bali wapate uzima wa milele. Mara nyingi tunafikiri kupenda ndugu zetu ni kuwapa mahitaji yao tu, hili ni kosa, kwani hitaji la kila binadamu ni kumfahamu Yesu na kuwa Naye milele. Je, wewe una uwezo wa kutembea kilometa 10 kwa siku? Anza kulifanyia mazoezi hili, litakusaidia kama mmishenari wa Bwana kutokuwa goigoi!

Alipoingia Petro, Kornelio alienda kumlaki, na kumwangukia miguu akimsujudia, lakini Petro akamwambia "Simama mimi nami ni mwanadamu" Ni Mungu tu anapaswa kusujudiwa, na hata si Malaika. Akizungumza na kuingia ndani, akaona watu wengi wamekusanyika. Alipotambulishwa, aliwaambia, "Wote hapa mnajua ya kuwa si halali kwa Myahudi ashirikiane kwa kula au kumtembelea mtu aliye wa mataifa mengine, lakini Mungu amenionya sina haki kumdharau au kumwita mtu awaye yote mchafu wala najisi, ndiyo maana nimekuja nilipoitwa, sikukataa, basi

nawauliza, ni neno gani mliloniitia?"

Kornelio naye akamweleza yaliyomtokea upande wake. Alimwambia kwamba siku tatu zilizopita aliona maono, kama saa tisa wakati akisali nyumbani mwake. Alimwona malaika mwenye nguo zinazong'ara na akamwambia "Kornelio Dua zako zimesikiwa na Mungu, na sadaka zako, na sadaka zako zimepokelewa na zinakumbukwa mbele ya Mungu." Akaendelea kusema Malaika alimwambia atume watu kumwita Petro, na akaambiwa alipo, na kwamba Atakapokuja atasema nawe. Kornelio akasema akatuma watu "nawe umefanya vyema kuja, basi sisi sote tupo hapa mbele za Mungu, tunangoja kusikia chochote ambacho Mungu amekwambia utuambie." Watu hawa walikuwa na kiu, na utayari wa kusikiliza na kufanya vile Mungu anataka.


*Maombi ya Nehemia yaliimarishwa na Kusudi Imara—Kuna hitaji la kuwa na akina Nehemia katika kanisa leo,—sio watu wanaoweza kuomba na kuhubiri tu, bali watu ambao maombi na mahubiri yao yameimarishwa kwa kusudi thabiti na lenye maazimio yenye shauku.
------------------------

Malaika alimwambiaje Kornelio? Petro alipata ndoto gani? Kwa nini Malaika wanakataa kusujudiwa? Twapasa kufanyeJe ili Mungu azisikie dua zetu? Petro alipataje Mafundisho kwamba Mungu si wa taifa moja tu?

**SIKU YA 306.**
**(Novemba 1)**

# Hakika Mungu hana upendeleo.


**Matendo 10.**



Hapo ndipo Petro alifungua kinywa na kusema "hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo, bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na Yeye." Akasema Neno lile alilowapelekea wana wa Israeli akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu Kristo, Ndiye BWANA wa wote, jambo lile ninyi mmelijua, lililoenea katika Uyahudi wote likianzia Galilaya, baada ya ubatizo aliohubiri Yohana. Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu Naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja Naye.

Petro akasema wao ni mashahidi, walimwona, walimsikia na walimgusa. Waliishi Naye akitenda yote kwa miaka mitatu na nusu, na Wayahudi katika Yerusalemu walimwua na kumtundika mtini, alikufa na Mungu alimfufua siku ya tatu. Baada ya kufufuka akamjalia kudhihirika. Hakuonekana kwenye kadamnasi kubwa za watu ila kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na Mungu, kama Petro na wengineo. Hawa walikula, na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka kwake kutoka wafu. Petro akasema Yesu aliwaagiza wamhubiri kwa watu na kushuhudia kwamba Yeye Ndiye Masihi aliyeamriwa na Mungu awe mhukumu wa walio hali na wafu. Manabii wote humshuhudia Yesu, na ni kwa Jina Lake tu, kila amwaminiaye, hupata ondoleo la dhambi.

Petro akimaliza tu kusema vile tu, Roho Mtakatifu akawashukia wote waliokuwa wanamsikiliza. Wale Wayahudi waliokuwa pale walishangaa kwamba Mungu aweza kuwapa Roho Mtakatifu watu wa mataifa, wakashangaa watu wakimsifu Mungu, tena wakawasikia wakinena kwa lugha mbali mbali kumhubiri Mungu. Hakika Mungu ni wa watu wote, si wa kabila, nchi, rangi, jamaa na lugha fulani tu. Petro akasema "Twawezaje kuwazuia watu hawa wasibatizwe na wamepokea Roho Mtakatifu kama vile sisi tulivyopokea wakati wa Pentekoste."



Akaamuru wabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo, ndipo wakamsihi akae siku zaidi, baada ya kuwabatiza. Mitume na Wayahudi wengine walipata habari kwamba watu wa mataifa wamepokea Neno la Mungu. Petro alipoenda Yerusalemu wale Wayahudi na waliotahiriwa, wakashindana naye, wakisema "uliingia kwa watu wale Wayahudi wasiotahiriwa ukala nao." Petro akaanza kuwaeleza kwa taratibu yale yaliyotokea, kuanzia njozi yake, mpaka safari yake, mpaka kukutana na Kornelio, na kumwagiwa kwa Roho Mtakatifu, hata kunena kwa lugha.

Kisha Petro akasema alikumbuka Mwalimu wake Yohana Mbatizaji alibatiza ubatizo wa maji na toba, ila sisi "alitupa kubatiza ubatizo wa Roho Mtakatifu." Akamalizia kuwaambia Wayahudi, ikiwa Mwenyezi Mungu amewapa wao karama ile ile aliyowapa Wayahudi na watu wa mataifa, mimi ni nani niweze kumpinga Mungu?" Wayahudi waumini waliposikia hayo walinyamaza na wakamtukuza Mungu wakisema "Kumbe basi Mungu amewajalia watu wa mataifa mengine pia uwezo wa kutubu na kuokolewa kwa kupata uzima wa milele." Imani kwamba mtu asiye Myahudi hawezi kuingia kwenye nyumba ya Myahudi au hawezi kupokea Roho wa Mungu ikafa.

Petro alikuwa muumini mzuri, hakuwahi kula nyama najisi kama dubu, simba, nguruwe, kaa, panya, paka au punda. Alipokuwa mwanafunzi wa Yesu aliona Yesu na mitume hawakula hivi vitu, na ndiyo maana akashangaa njozi ile ina maana gani? Ila alipoitwa na watu wa mataifa aligundua ujumbe Mungu alimpa si kula nyama ambazo si njema kwa afya, bali awe na upendo kwa kuwambia Warumi na watu wote habari njema za ufalme ili wasipotee bali wawe na uzima wa milele.

Awali binadamu alipoumbwa alipewa mimea tu kuwa chakula chake (Mwanzo 1:29). Baada ya dhambi na gharika, mimea ilikufa, ndipo Mungu alimpa Nuhu na familia yake kula wanyama safi ambao wasingekuwa na madhara kwa afya zao, ila alipewa masharti ya namna ya kuwatumia hao nao. Nuhu kwenye safina hakula nyama na kama angekula wanyama hao najisi wasingekuwepo leo, maana walikuwa wawili tu. Ila walipewa masharti hata kwa wanyama wale wanaofaa kula ila wasile kibudu, mafuta au damu ya mnyama- Soma Walawi 11.


*Kila asubuhi chukua muda kuanza kazi zako kwa ombi. Usifikirie kuwa huku ni kupoteza muda; kwani ni muda ambao utaishi kwa nyakati za milele. Kwa njia hii mafanikio na ushindi wa kiroho utaletwa. Mwili wako utajibu mguso wa mkono wa Mwalimu Mkuu. Hakika kuomba baraka ya MUNGU kunastahili wakati wetu, na kazi haiwezi kufanywa kwa usahihi isipokuwa ina mwanzo sahihi.
-----------------------------

Maswali: Hakika natambua Mungu hana upendeleo ina maana gani? Mungu angekuwa na upendeleo au ubaguzi kama mimi ingekuwaje? Kwa nini walishangaa Roho Mtakatifu alipowashukia watu wa mataifa? Kwa nini waliwabatiza wale watu waliomwamini Kristo? Kwa nini Petro hakutaka kumpinga Mungu?

**SIKU YA 307.**
**(Novemba 2)**

# Petro atolewa na Malaika gerezani.

**Matendo 11-12.**



Waumini waliotawanyika baada ya dhiki iliyotukia kwa Stefano kuuwawa waliendelea kusafiri Foinike, Kipro, Antiokia, Kirene na mahali pengine wakihubiri Neno la Mungu, ila kwa Wayahudi peke yao. Waliendelea kuwa na umoja na kusaidia, hakuna aliyekosa mahitaji yake au kupata shida bila waumini wengine kumsaidia. Ila wale Wayahudi waliofikiri hamu ya kumhubiri Yesu itazimia, waliendelea kutesa waumini au wanafunzi wapya wa Yesu, wakiwa na mioyo migumu ya mawe, na macho yao yalipofuka wasitake kuijua ile Kweli. Mkono wa Mungu ukaendelea kuwategemeza Wakristo hawa wapya, wengi hata wale waliofikiri kwamba kumwamini Yesu ni kuwa mwendawazimu wakajiunga nao.

Wale watu wa Kisiwa cha Kipro na Kirene walipofika Antiokoa, Syria, wakasema na Wayahudi wa Kiyunani habari njema bila woga na mkono wa BWANA ukawaongoza wakapata watu wengi kumwelekea BWANA. Habari hizi zikafika masikioni mwa watu kanisani Yerusalemu, wakamtuma Barnaba/Barsaba, mwana wa matumaini aende Antiokia. Naye alipokwisha kuona neema ya Mungu imewabadilisha watu hawa, na watu wengi wamemwamini aliwatia moyo wakae katika imani ya ile Kweli ya BWANA kwa mioyo yao yote.

Barnaba alikuwa mtu mwema, aliyejaa Roho Mtakatifu na imani; watu wengi wakaongezeka kwa BWANA kupitia kazi yake. Akaenda Tarso kumtafuta Sauli ili aje kumsaidia, wakapanda meli na kwenda Antiokia. Wakakaa kule kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Huu ukawa mwanzo wa mahusiano kati ya Paulo na Barnaba ya kufanya kazi kwa pamoja kwa miaka mingi kati ya watu wa mataifa mbali mballi. Watu wa Antiokia wakiona upendo, wa Barnaba na Paulo, walipomhubiri Kristo, walianza kuwaita wafuasi wa Yesu Wakristo kwa mara ya kwanza, ikiimanisha wafuasi wa Yesu Kristo. Leo, sisi ni wafuasi wa Yesu Kristo, tunaiga tabia Yake, tunafuata nyayo Zake.

Hapa ndipo Neno la Kiyunani Kristo likaanza kutumika, maana Masihi ni Neno la Kiyahudi. Neno hili lina maana ya "Mpakwa mafuta au Mteule wa Mungu." Hata leo sisi tunaitwa Wakristo tunapomkubali na kumwamini Yesu BWANA aliyekufa msalabani kwa ajili ya wokovu wetu Kisha kafufuka. Hatuwezi kuwa Wakristo bila kumfuata Kristo kwa moyo wetu wote. Yeye ndiyo kiini, chanzo na kinara cha imani yetu. Siku za nyuma watu hawakumjua Yeye ila alikuja akaishi na kujifunua kwa watu. Hata leo wengine hawamjui. Hebu kwa upendo na huruma, uwaambie habari hizi maana "Uzima wa milele ni kumjua Mungu wa Pekee na Yesu Kristo aliyemtuma." Yohana 17:3. Wakimjua ndiyo watakuwa na uzima wa milele na pia imani inakuja kwa kusikia Neno la Mungu na si kwa kutosikia, na kila mtu Mungu amempa kiasi fulani cha imani. Tunapopenda watu kwa upendo wa Kweli, hatutaki waangamie siku ya kiyama.

Siku zile manabii walienda Antiokia na mmoja wa manabii aitwaye Agabo akasimama akanena yale aliyoonyeshwa na Roho Mtakatifu kwamba njaa kubwa itakuja katika sehemu kubwa ya dunia, nayo itatukia katika siku za Mtawala wa Rumi Kaisari Klaudio. Wale waumini kila mtu kwa kadiri alivyofanikiwa wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi, basi wakawapelekea wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli. Panapo majira hayo Herodi Agripa I, mfalme ambaye baba yake mkubwa alikuwa Herodi Antipasi aliyemwua Yohana mbatizaji, na babu yake ndiye Herode aliyeua watoto wa Bethlehemu, akanyosha mkono wake kuwatenda mabaya baadhi ya watu wa kanisa; akamwua Yakobo mtume ambaye ni ndugu yake Yohana wale wana wa Ngurumo kwa upanga.

Hapa ilikuwa kama miaka kumi toka kupaa kwa Yesu. Akaona Wayahudi wale wa baraza la Sanhedrini wamefurahia Ukatili huo akaendelea kutesa watu, akamshika Petro siku hizo za Pasaka. Akifikiria huyu ndiyo mkuu wa 'genge' hili la Wahubiri wa injili ya Yesu. Akamweka Petro gerezani, na kuamrisha vikosi vine vya askari vimlinde ili asitoroke. Akitaka baada ya Pasaka amtoe na kumweka mbele ya watu kisha amwue.

Petro alishinda gerezani, akifikiria kwamba huu ndiyo mwisho wangu wacha niungame mapungufu yangu kwani maisha yangu yatakoma kama ya Yakobo. Kanisa lilikuwa likimwomba Mungu kwa juhudi kwa ajili yake. Herode alipotaka kumtoa, amlete mbele za watu na kisha amwue, usiku ule kabla hajafanya vile, Petro akiwa amelala katikati ya askari wawili na amefungwa minyororo miwili, miguuni na mikononi na walinzi mbele ya mlango wakalinda gereza. Mara Malaika wa BWANA akasimama karibu yake. Nayo nuru ikamulika, na malaika akamgusa Petro ubavuni amwamshe, akisema "ondoka upesi." Minyororo ikafunguka na kuanguka chini, kisha malaika akamwambia ajifunge mkanda na nguo zake, pia viatu, naye akatekeleza Maagizo akamfuata yule Malaika.

Akatoka nje wala hakujua kama ni kweli au yupo ndotoni, au kwenye maono. Walipita mlango wa kwanza na wa pili, akiwa na malaika, kisha walikuja mlango wa chuma wa kuingilia mjini, nao ukafunguka wenyewe bila sauti. Wakatoka nje na Malaika akamwacha. Petro akapata ufahamu kwamba "kumbe, Mungu amenitumia Malaika kunitoa kwenye mkono wa Herodi na Wayahudi wanaotazamia mimi kuuwawa

leo." Alifikiri haya akitembea na akawa amefika nyumbani mwa Mariamu mamaye Yohana Marko. Nyumba hii pengine ndiyo ile ambayo ndimi za moto za ishara ya Roho Mtakatifu ziliwatokea mitume.

Watu wengi walikuwa wamekutana wakimwombea Petro, kwani walihofu yaliyompata mtume Yakobo yatatokea kwa Petro kukicha. Petro alipopiga hodi, Kijakazi Roda aliendа mlangoni na alipotambua sauti ya Petro, alifurahi na kupiga mbio kuwaambia wengine kwamba Petro yupo mlangoni. Japo walikuwa wanamwombea Mungu afanye miujiza aponyoke makuchani mwa Herodi, hawakuamini, kwamba Mungu anajibu maombi! Wakamwambia alipokazana 'una wazimu wewe'. Wengine waliamini ni malaika wa Petro. Petro akaendelea kugonga, gonga ndipo wakafungua na kustaajabu.

Akawapungia na kuwaeleza jinsi Mungu alivyomtoa gerezani. Akawaambia wampashe Yakobo, ambaye alikuwa ndugu wa Yesu, na mkuu wa baraza la mitume na wale ndugu habari hizi. Akaondoka kwenda pengine kuhubiri, bila kupoteza muda wake wa kuwa huru, akiwahadithia wale wasiojua kisa cha Yesu. Hata nasi tumefunguliwa kutoka minyonyoro ya Shetani, ili tuweze kutangaza habari njema. Maombi yanaleta tofauti kubwa, hebu na tubebe kikapu chetu chenye haja zetu zote za moyo, wala tusibakize lolote linalotupa wasiwasi au huzuni na tumpelekee Yeye! Pengine hata Paulo alipowekwa kifungoni, kanisa lingemwombea angetoka, ni nani ajuaye yale mambo tuliyoyakosa kwaajili ya kutoomba? Tumeambiwa "hamna kwasababu hamkuliomba hilo!". Sasa sisi tusikose lolote jema eti kwa vile hatukuomba. Je, unaafikiana nami katika hili?

Asubuhi askari walifadhaika, "imekuwaje Petro alitoka tena? Herodi akamtafuta Petro asimwone na mwishowe akawaua wale walinzi. Petro akatelemka Uyahudi, na kukaa huko. Kisha Herode aliwakasirikia Wasidoni na Tiro, nao wakamwendea kwa nia moja ili wafanye urafiki naye, na kutaka amani, kwa maana nchi yao ilipata riziki ya chakula, toka kwa mfalme Herode. Siku iliyopangwa Herode alivaa mavazi ya kifalme, na kutoa hotuba kwa mabalozi wa nchi hizo. Watu wale waliowakilisha nchi zao, kwa kupatana naye walimvimbisha kichwa kwa kelele za kumfurahisha (kumshenteka) au kumsifu ili wasipoteze riziki zao, wakisema "ni sauti ya Mungu na wala si binadamu."

Herode hakukanusha maneno haya. Japo alijua yeye si kitu chochote bali ni kiumbe tu, yaani hakumpa Mungu utukufu. Japo alikuwa Myahudi aliyelelewa toka utoto akijua Mungu ni mmoja tu, na binadamu wote ni maua ya kupita. Akakubali watu wamwabudu. Alipomaliza kukufuru tu, wale Wasidoni wasiojua kitu, hatuambiwi kwamba waliangamia. Bali mara ile Malaika wa Bwana akampiga Herodi na chango la minyoo, tumbo likaoza, kwa kuwa hakumpa Mungu utukufu. Basi Herode alikufa kifo kibaya cha kuoza tumbo. Japo Wakristo hawa wa mwanzo walipata mateso, Neno la Mungu likazidi kuenea na miujiza mingi ikatendeka.

*Katika kumfuata Kristo, ukimtazama Yeye ambaye Ndiye Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yako, utahisi kuwa unafanya kazi chini ya jicho Lake, kwamba unashawishiwa na uwepo Wake, na kwamba Anajua nia zako. Katika

kila hatua utauliza kwa unyenyekevu: Je! Hii itampendeza Yesu? Je! Itamtukuza MUNGU? Asubuhi na jioni sala zako za dhati zinapaswa kupaa kwa MUNGU kwa ajili ya baraka na mwongozo Wake. Maombi ya Kweli hujitegemeza kwa Muweza na hutupatia ushindi. Akiwa amepiga magoti yake Mkristo hupata nguvu za kushinda vishawishi.

-------------------------------

Maswali: Kazi ya kanisa ni nini? Unajuaje kama kanisa lako halifanyi kazi yake? Petro alitokaje gerezani? Mtume wa kwanza kufa kwa ajili ya Kristo ni nani? Kwa nini tumbo la Herodi lilioza? Je watu wakikusifu kama walivyomsifu Herodi ufanyeje? Kwa nini Herode alimwua mtume Yakobo? Tunawezaje kuepuka tumbo kuoza leo?

**SIKU YA 308.**
**(Novemba 3)**

# Wayahudi wakataa injili, Ukristo waenda kwa mataifa.

**Matendo 13-14.**

Barnaba na Sauli wapomaliza huduma yao, wakarejea Yerusalemu. Hapa wakamchuka Yohana Marko kwenda kule Antiokia kilomita kama 350, wakitumwa kama wamishonari wa kwanza. Hapa walikuwepo manabii na walimu wa Kikristo waitwao Barnaba, Simeoni mtu mweusi, Lukio Mkirene Mwafrika wa Libya, na Manaeni aliyekuwa ndugu wa tumbo moja na mfalme Herode na Paulo. Walifanya ibada na kufunga, Roho wa Mungu akawaagiza wawatenge Barnaba na Sauli kwa kazi aliyowaiitia. Wakawawekea mikono watu hawa na kuwaacha waende zao.

Kuwawekea mikono ilikuwa ishara ya kumwomba Mungu awape baraka za pekee katika kufanya kazi Yake, na kuonyesha kwamba wao kama watenda kazi katika BWANA wanawaunga mkono watenda kazi wenzao. Wakiongozwa na Roho walienda Seleukia, hata kisiwa cha Kipro. Wakaenda Salami, wakahubiri kwenye masinagogi ya Wayahudi na Yohana Marko. Siku zile za usafiri mgumu, hakukuwa na treni, magari, ndege au meli za kasi. Mitume walitembea kwa miguu na kupanda merikebu ili wengi wabarikiwe kumjua Yesu. Paulo alifanya safari kuu tatu, akiendea miji mbali mbali (tazama ramani). Ila kuna pia safari ya nne. Hapa ni safari yake ya kwanza, Safari yake ya mwisho ndiyo ilimchukua Rumi.

Katika kazi hii ya umishonari. Mitume walikutana na shida nyingi, maana Shetani hutumia mtu yoyote anayetaka kutumiwa naye kuirudisha nyuma kazi ya Mungu. Walipofika Pafo waliona mchawi wa uongo Myahudi aitwaye Bar-yesu au Elima. Huyu alikuwa na gavana wa pale aitwaye Sergio Paulo, mtu mwenye akili nyingi. Gavana huyu aliwaita Barnaba na Paulo akitaka kulisikia Neno la Mungu aokolewe, ila Bar-Yesu akashindana nao, akitaka kumkataza yule gavana asimpokee Yesu na kupindisha pindisha ajenda. Paulo akijaa Roho Mtakatifu alimkazia macho akasema "Ewe mwenye kujaa hila na uovu wote mwana wa Ibilisi na adui wa haki yote, huachi kuzipotoa njia za BWANA zilizonyoka? Angalia mkono wa Bwana u juu yako nawe utakuwa kipofu kwa muda." Akawa kipofu, na ikabidi mtu amwongoze. Yule gavana alipoona hayo aliamini na kuyastaajabia mafundisho ya BWANA. Tunaposoma kitabu cha Matendo Paulo alipokutana na wajina wake Paulo (namesake), ndipo alianza kuitwa jina hili, mpaka mwisho.

Paulo na wenzake wakang'oa nanga na kwenda Pafo, Perge na Pamfilia. Yohana Marko akawa amechoka na maisha magumu ya uinjilisti wa bila mshahara, yaani alikuwa mlei, hatari, shida nyingi na mateso. Akarudi zake Yerusalemu. Wengine wakaenda Antiokia, Pisidia na kuingia katika sinagogi siku ya Sabato. Shemashi

Nicolas alitoka sehemu hizi za Uyunani. Baada ya torati kusomwa sinagogini walituma wakuu kuwaambia wazungumze nao wakiwa na "Neno la kuwafaa watu, lisemeni." Paulo akasimama na kumwelezea Yesu, Masihi kama Yule aliyeahidiwa. Alianza kuelezea historia ya wana Israeli mababa Imani kama Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Kisha utumwa wa Misri, na kisha jangwani miaka 40.

Akaeleza mataifa 7 yalivyopigwa Kanani ili warithi nchi ya Kanani kwa muda wa miaka 430. Kisha waamuzi, na nabii Samweli mwamuzi wa mwisho. Kisha Sauli walipotaka mfalme kama wengine, na Daudi "aliyependeza moyo wa BWANA na kufanya mapenzi Yake yote." Akaeleza unabii kwamba Daudi ataleta uzao wa Mwokozi, yaani Yesu kama alivyoahidi Masihi. Akawaelezea kwa undani kwamba Yesu ni Mwana wa Daudi wa unabii. Ndipo aliporudia kuwafundisha maana ya ubatizo wa Yohana mbatizaji wa maji na toba kujitayarisha na Masihi.

Akaeleza jinsi uzao wa Ibrahimu na wote wa Israeli walivyokosa kutambua kwamba Masihi ni Yesu, wakamhukumu bila sababu hata Pilato alipowaambia Yesu hana hatia. Wakamsulubisha, na kumtoa katika ule mti wamzike, Naye akafufuka katika wafu baada ya siku tatu. Akaonekana kwa siku 40 kwa wanafunzi na wengine ambao ndiyo mashahidi wake. Paulo akasema "na sisi tunahubiri habari njema ya ahadi ile, mliyopewa na mababa kwa watoto wenu kwa kumfufua Yesu" na Mungu aliahidi akisema "Nitawapa ninyi Mambo Matakatifu ya Daudi yaliyo amini."

Akawaambia Daudi alipomtumikia Mungu alilala usingizi wa mauti. Ila Yesu alimfufua "ijulikane leo ndugu, tunahubiri habari za msamaha wa dhambi, na kila amwaminiaye uhesabiwa haki, kwa yote asiyoweza kuhesabiwa haki katika torati ya Musa." Akawasihi wasidharau, au wasingoje kusimuliwa sana, kama Habakuki 1:5 isemavyo bali wampokee Yesu na kuacha mapokeo ya Musa ya kafara, kwa kuwa Yesu ameshakufa, Kafara ile halisi ya Kweli kwa ondoleo lao la dhambi

Wale watu wakawasihi wakae mpaka Sabato ya pili tena. Sabato nyingine wakafumuka watu wengi sana Wayahudi, na waongofu. Watauwa wengi wakakubali Maneno ya Injili toka kwa Paulo na Barnaba; ila Wayahudi wakaona wivu walipoona Paulo anapendwa na watu wengine wanamkubali Yesu na kupata wokovu. Wakaanza kupinga pinga yaliyonenwa wakibishana na kuwatukana watumishi wa Mungu ili kupotezea lengo. Hapo ndipo watumishi wa Mungu hawa walisema "Ilikuwa lazima Neno la Mungu lianze kusemwa kwanza kwa Wayahudi ila mnalitupa mbali, na kujiona nafsi zetu hazistaili uzima wa milele, basi tutawageukia mataifa, maana nabii Isaya alisema nimekuweka uwe nuru ya mataifa, upate kuwa wokovu hata miisho wa dunia'.

Basi walikung'uta mavumbi, ya miguu yao na kuendea mataifa mengine. Na wale wa mataifa walifurahi na kulitukuza Neno la BWANA, kwa kuwa Mungu aliwakusudia nao pia wapate uzima wa milele. Neno la BWANA likaenea katika nchi yote. Wayahudi wanaume walipoona wanawake wao, hasa wale wenye cheo wanampokea Yesu Masihi, wakawatisha, na kuwachochea wawaudhi Paulo na Barnaba, na kuwafukuza mipakani mwao. Wakakung'uta mavumbi ya viatu vyao na kwenda Ikonio. Waumini na wanafunzi walijaa furaha na Roho Mtakatifu.


*Tenga muda kila siku kwa ajili ya maombi — Wale ambao watavaa silaha zote za MUNGU na kutenga muda kila siku kwa ajili ya kutafakari na kufanya maombi na kusoma Maandiko wataunganishwa na mbingu na watakuwa na mvuto uokoao, na unaobadilisha kwa wale wanaowazunguka. Mawazo makuu, matamanio bora, ufahamu dhahiri kuhusu ile Kweli na wajibu kwa MUNGU, haya yote yatakuwa yao. Watakuwa wana shauku ya kuwa na usafi wa moyo, kuwa na nuru, kuwa na upendo, na kuwa na neema zote zitokazo mbinguni. Maombi yao ya bidii kabisa yatapenya ndani ya pazia. Kundi hili litakuwa na ujasiri mtakatifu mbele ya Yeye Asiye na kikomo. Watahisi kuwa nuru na utukufu wa mbinguni upo kwa ajili yao, na watasafishwa, watainuliwa, wataboreshana kuadilishwa na uhusiano huu wa karibu na MUNGU. Huo ndio upendeleo walionao Wakristo wa kweli.
---------------------------

Maswali: Kwa nini Bar yesu alipofuka macho? Paulo na Barnaba waliwekewa mikono kwa ajili gani? Kwa nini mitume walikung'uta miguu yao? Tunajifunza nini toka kwa Yohana Marko? Kwa nini Paulo alipenda kueleza historia ya Wayahudi? Kwa nini waumini walimtuma Barnaba Antiokia?

**SIKU YA 309.**

# Paulo apigwa mawe Lystra.

**Matendo 14**



Walipofika Ikonio, wakafanya kama vile walipoenda Antiokia, wakaingia katika sinagogi. Kundi kubwa la Wayahudi na Wayunani likaamini. Lakini Wayahudi wasioamini wakachochea jumuiya ya watu wa mataifa na wengine kuwatia nia mbaya juu ya wahubiri wa injili. Kila mahali pana watu wa kuleta vurugu na shida kwenye kazi ya Mungu.  Paulo na Barnaba walikaa hapa wakanena kwa ushujaa mwingi Neno la Neema ya BWANA Yesu Kristo. Mungu akawajalia ishara na maajabu yatendeke mikononi mwao. Watu wakagawanyika wengine upande wa Wayahudi na wengine mitume, Wayahudi wakawapiga watu kwa mawe. Wahubiri hawa wakakimbia Derbe, Listra, Likaonia, na nchi za kando na kukaa kule wakihubiri injili. Hizi ndizo nchi za Ulaya walizozifikia kwanza.

Kule Listra kulikuwa na aliyezaliwa kiwete cha udhaifu wa miguu, asiyewahi kutembea na alipomsikia Paulo akihubiri alihudhuria. Paulo akimkazia macho na akamwuliza kama ana imani ya kuponywa, kisha akamwambia asimame kwa sauti kuu. Ndipo aliposimama na kutembea kwa haraka. Watu walipoona walistaajabu na kusema kwa lugha yao "Miungu wametushukia kwa mfano wa wanadamu."

Wakamwita Baranabas Zeu, mungu wao maana alionekana ana sura ya kifalme na Paulo Herme, kwa sababu alikuwa ndiye mnenaji wa yule mungu Zeus. Bila Paulo na Barnaba kujua walileta ng'ombe na taji za maua mlangoni wakitaka kuwatolea dhabihu.

Mitume walipopata habari walirarua nguo zao waaenda mbio na kusema kwa makutano "mbona mnafanya haya? Sisi nasi tu wanadamu kama ninyi. Twawahubiri habari njema mgeuke toka mambo ya ubatili ya kuabudu miungu na kumwelekea Mungu aliye hai, aliyeumba kila kitu, iwe ni mbingu, nchi, bahari na vyote. Zamani aliacha mataifa waende njia zao za giza au ujingani, lakini hakuwaacha bila kuwapa ushuhuda kwamba ni Yeye aliwatendea mema yote, iwe ni mvua, mavuno, chakula au furaha. Basi makutano wakaacha kutoa ile kafara.

Yale makutano ya Wayahudi toka Ikonio na Antiokia walifika na kuwashawihi watu wawapige mawe wahubiri wa Mungu. Wakamburuta Paulo nje ya mji na kumpiga mawe, na huku wakidhani amekufa wakaenda zao. Waumini au wanafunzi wa Maandiko walimzunguka Paulo, na wakaona mwujiza aliposimama, akaenda na Barnaba Derbe. Pale walihubiri na kupata wanafunzi wengi kwa Yesu. Kisha wakarejea Listra, Ikonio na Antiokia. Waliwaimarisha wanafunzi na kuwaonya wakae watika imani na kujua kwamba kila muumini "imempasa kuingia ufalme wa Mungu wa njia ya dhiki nyingi." Kila kanisa waliloanza walichagua wazee wa kanisa kusimamia, wakawawekea mikono ya BWANA waliyemwamini, watunze makanisa hayo kama wachungaji.

Paulo aliandika barua za kichungaji kwa Timotheo, na Tito walipokuwa wanachunga makanisa. Barua hizi zapaswa kusomwa na kila mchungaji, mshiriki na muumini ili ajue jinsi ya kuenenda katika njia ya Kristo. Waliendelea na safari kuhubiri miji ya Pisidia, Pamfilia, Perge na Atalia. Kisha wakaenda Antiokia, wakaombewa kule neema ya Mungu kwa kazi waliyomaliza kuifanya. Hapa waliwaambia waumini wakutanike na kuwaeleza mambo yote Mungu aliyofanya pamoja nao, na kwamba Mungu "amewafungulia mataifa mlango wa imani. Wakaa pale kwa muda. Kazi ya Paulo na Barnaba ilikuwa na dhiki za ajabu. Kazi hii iliwezekana tu kwa ajili ya neema za Mungu, yaani ile imani waliyokuwa nayo na upendo wao kwa Mungu na watu.

Ujasiri wao ndiyo umetuletea injili hata leo kwetu hapa Afrika. Hebu tuombe nasi tupate huo mguso au ambukizo ili tuwapelekee wengine habari njema.

*Kutafakari nadharia tu bila vitendo halisi haitoshi; shughuli au utendaji mwingi pia hautoshi; vyote viwili ni muhimu kwa uundaji wa tabia ya Kikristo. Nguvu inayopatikana katika maombi ya dhati, na ya siri, hututayarisha kustahimili vivutio na vishawishi vibaya kwenye jumuiya. Na bado hatupaswi kujitenga na ulimwengu, kwani uzoefu wetu wa Kikristo unapaswa kuwa nuru ya ulimwengu. Jamii ya wasioamini haitatudhuru ikiwa tutachangamana nao kwa kusudi la kuwaunganisha na Mungu na kuwa na nguvu za kutosha kiroho kuhimili ushawishi wao.

----------------------------

Maswali: Kwa nini "imetupasa kuingia ufalme wa Mungu kwa nia ya dhiki nyingi?" Barnaba na Paulo walipobatizwa majina ya miungu walifanya jambo gani? Kiwete wa Listra alipopona watu walisemaje?  Paulo alitendewa jambo gani Lystra? Ni barua gani ya Paulo haikushugulikia matatizo bali ilikuwa ikiwapongeza tu na kusaidia mawasiliano ya kazi?

**SIKU YA 309.**
**(Novemba 4)**

# Baraza la Mitume laandika barua ihusuyo wamataifa wanaomwamini Yesu.

**Matendo 15.**



Wakristo hawa wa kwanza walikuwa mafarisayo wa Kiyahudi kabla ya kupokea imani hiyo mpya ya ukristo. Watu hawa walifikiri watu wa mataifa wakimkubali Kristo kama hawa wa Antiokia, imewapasa waanze kutunza mapokeo na mila za kiyahudi. Mila hizo ni kama kutahiriwa, siku kuu za Kiyahudi, na mengineyo, yaani yote yale yaliyotunzwa kabla ya Yesu kutoa kafara Yake msalabani. Walitaka watu wawe Wayahudi kwanza ndipo wawe Wakristo. Wale wa mataifa waliona kwamba wamempokea Yesu na kupokea Roho Mtakatifu, hivyo hawakuona haja ya mapokeo ya Kiyahudi yaliyopitwa na wakati au yasiyo na uhusiano na kumwabudu Mungu na Mwana Wake.

Wakati huo walishuka watu kutoka Uyahudi wakifundisha kwamba "mtu usipotahiriwa kwa desturi ya Musa huwezi kuokoka." Paulo na Barnaba walihojiana na watu hawa kwa mjadala mgumu sana; ndipo watu walio pale wakaamuru Paulo

na Barnaba na wengineo, waende Yerusalemu, kwa mitume na wazee kwa habari ya swala hilo wakaliweke sawa ili watu wasichanganywe na fujo za watu walioshikilia sheria ya Musa na kutahiriwa. Wakisafirishwa na kanisa walipita Foinike, na Samaria, wakitangaza habari za kuongoka kwao. Watu wa mataifa, wakaburudisha mioyo ya ndugu katika Kristo kwa zile habari njema. Walipofika Yerusalemu wakakaribishwa na kanisa la mitume na wazee na wakawaeleza yale Mungu aliyoyafanya pamoja nao walipotembea umbali mrefu zaidi. Wakaeleza baadhi ya mafarisayo wamedai ni lazima kuwatahiri mataifa na kuwaagiza kushika torati ya Musa.

Mitume na wazee waliita baraza kufikiri neno hilo, na baada ya hoja nyingi, Petro alisimama na kusema "Ndugu zangu mwajua ya kuwa si siku nyingi Mungu alichagua miongoni mwetu mataifa walisikie Neno la injili na kuliamini." Akaeleza kisa cha Kornelio walichokifahamu. Mungu ajua mioyo ya watu, amewashuhudia na kuwapa Roho Mtakatifu kama alivyotupa sisi, wala hakuna tofauti, akiwasafisha mioyo yao kwa imani. Akawauliza waumini Wayahudi "sasa mbona mnamjaribu Mungu na kuweka kongwa juu ya shingo za waumini wapya wa mataifa, ambalo baba zetu wala sisi hatukuweza kulichukua?

Mkutano wote ukanyamaza wakawasikiliza Barnaba na Paulo wakiwapasha habari za ishara ya maajabu ambayo Mungu aliwafanyia wale watu wa mataifa waliompokea Mungu katika safari yao ndefu. Mwenyekiti Yakobo au kwa jina jingine James, akawapa muda wa kujadili na kutoa maoni yao. Wakimaliza kusema au kujadili mengi, Yakobo ambaye ni ndugu wa Yesu, ndiye aliyekuwa mkuu wa baraza, naye akaweka hitimisho. Alisema "Ndugu zangu Simoni Petro alitueleza hapo awali jinsi Kornelio na watu wa mataifa walivyoangaliwa na Mungu, na kwamba amewachagua watu hao kwa jina lake, na nabii Amosi alitueleza kwamba ataijenga nyumba ya Daudi iliyoanguka na kuisimamisha ili wanadamu waliosalia wamtafute BWANA na mataifa yote ambayo Jina Lake limetajwa kwao."

Yakobo akasema kwa hayo Mungu aliyowafunulia wa mataifa imeonyesha wazi kwamba Mungu ni wa wote. Hivyo wasiwataabishe wa mataifa waliomgeukia Mungu, kwa mawe mazito vichwani mwao, bali wawaandikie waraka. Waraka huu uwaelekeze watu wa mataifa "wajiepushe mapokeo ya upagani kama vile uasherati, nyama za kibudu, au zilizongwa na damu, na mapokeo au mila za uchafu zisizopatana na maagizo ya Mungu. Pia tuwaambie wachukue muda kuijua torati, ambayo tunasoma kila wiki kwenye masinagogi yetu." Basi wakaamua yale waliyoafikiana nayo wayaweke kwenye maandishi. Maandishi ni muhimu sana, maana yanaleta mawazo yaliyojadiliwa kwenye karatasi ili wakienda mahali wasaidie wengine na kumbukumbu hiyo kutenda Mapenzi ya Mungu kwa amani na umoja. Siku hizi mikutano inarekodiwa na Youtube au Facebook!

Basi ikawapendeza mitume kuwapeleka wamishonari wa kwanza, rasmi kiofisi Antiokia pamoja na Paulo, Barnaba, Yuda aitwaye Barsaba, na Sila. Wakawapa barua iliyosema hitimisho walilofanya mitume ikisema hivi "Mitume na ndugu wazee, kwa ndugu zetu walioko Antiokoa, Shamu, Kilikia, na mataifa yote salamu. Kwa kuwa tumesikia ya kwamba Wayahudi fulani wamesumbua kwa maneno ya kupotosha roho zenu watu wa mataifa ya nje ya uyahudi; kwa mambo ambayo

sisi hatukuwaagiza, tumeona tuandike kwenu. Sisi tumeona vema na kupatana kwa moyo mmoja, katika baraza la mitume na waumini kuchagua wamishonari, kuwapeleka kwenu, pamoja na Barnaba na Paulo.

Hawa wamehatarisha maisha yao kwa ajili ya Jina la Yesu Kirsto, basi tumewatuma Yuda na Sila watakaowaambia maneno hayo hayo, kwa vinywa vyao. Imempendeza Roho wa Mungu na sisi tusiwatwike mizigo ila hayo ya lazima. Yaani mjiepushe desturi na mila za kipagani za kutoa sadaka kwa sanamu, na kutokula wanyama waliosongolewa, kuepuka uasherati, na uovu wote. Mkijizuia kwa hayo, mtafanya vyema. Wasalaamu, baraza la kanisa la Mitume, Yerusalemu."

Wakisha pewa ruhusa na baraza walienda Antiokia, wakakusanya waumini na kuwapa barua ile. Walipokwisha kuisoma wale waumini wa mataifa wakafurahi mno, kwa ajili ya ile faraja. Yuda na Sila ambao pia walikuwa manabii, waliwausia wale ndugu kwa mazungumzo mengi, wakawathibithisha au kuwaimarisha katika imani. Ila Sila, Paulo, na Barnaba waliamua kuendelea kukaa pale wakihubiri. Baada ya Muda Paulo alimwambia Barnaba warejee kwenye miji waliyohubiri ili kuwaimarisha waumini wapya na kuwalisha Neno la Mungu.

Barnaba akaazimu kumchukua Yohana Marko aliyekuwa mpwa wake mdogo, aende pamoja nao. Paulo hakupenda, maana Yohana Marko aliwatelekeza Pamfilia, kwa kuchoka maisha magumu ya kazi ya uinjilisti. Pakatokea kutoelewana kati yao, na wakatengana, kila mtu akienda mji wake kuhubiri. Zikawa timu mbili. Mashindano au mafarakano si mazuri kwa waaminio, ila huwa yanatokea. Basi pale yanapotokea yatafutiwe njia nzuri ya kutatuliwa, maana hakuna mtu anayeweza kukubalina na mwenziwe mara zote. Barnaba alifanya jambo zuri, kumpa nafasi nyingine kijana Marko ya kuimarika baada ya kurudi nyuma.

Hapo zamani za kale, Yerusalemu ilipokuwa ijengwe upya, nabii katika maono alimsikia mjumbe mmoja wa mbinguni akimwambia mwenzake, "Kimbia, ukaseme na kijana huyu." Zek 2:4. Na kwa hiyo, katika siku hizi zetu za mwisho, vijana wa kiume na wa kike kwenye harakati hizi za majilio ya Bwana, wamepewa sehemu muhimu ya kutenda katika tamthilia ya kufunga historia ya dunia. Bwana ameteua jeshi hili la vijana waliofunzwa ifaavyo, na watafanya ujumbe wa Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka ubebwe ulinwenguni kote kwa upesi!

Hebu kila ampendaye Mungu atoe nafasi kwa watoto na vijana wanapokosea, ili waweze siku moja kuwa watenda kazi watakaovuvia wengi kwa Kristo. Mungu akatumia mfarakano huu kufikia miji miwili kwa injili, japo lilikuwa jambo ambalo si jema Warumi 8:28. Lazima tujifunze kuwa wavumilivu na watoto na vijana maana Marko siku moja alikaa chini, na yale aliyojifunza akiwa na Petro na mitume wengine aliandika kitabu cha kwanza cha injili, kikaitwa Marko. Wengine husema hiki lilimsaidia hata Mathayo wakati anaandika kitabu chake chae Injili. Timu hizi mbili zikaombewa na Barnaba akamchukua Yohana Marko wakaenda Kipro (Cyprus), na Paulo akamchukua Sila wakaenda wakipita Shamu na Kilikia wakiimarisha makanisa.

Yohana Marko alikomaa na kuwa shujaa. Mara zingine Roho wa Mungu atatusaidia jinsi ya kushugulika na vijana kwa kuwaonyesha kwamba tunawaamini na hilo linaweza kuwatia moyo kutenda makubwa. Paulo katika barua zake anashukuru huduma za Yohana Marko katika kufariji, na ya kuwa alikuwa msaada mkubwa kwenye huduma yake. "Mlete Marko kwani ananifaa kwa utumishi." Hawa watu waliyasahau yaliyopita, na wakasemeheana ya zamani na kusonga mbele. Marko alijifunza kumtegemea Mungu na kukua kiimani. Basi ilikuwa vyema mjomba wake Baranaba alikuwa na uvumilivu kwake.

Watoto au vijana wana mengi mazuri kama vile nguvu za kufanya mambo na shauku isiyokua na madoa ya uzoefu wa zamani. Watu wazima wenye uzoefu mzuri wa kazi ya Mungu pia ni msaada wa kuwapa hekima au uzoefu vijana ili kufanya kazi, maana huyachuja mambo kwa umakini mkubwa zaidi. Ila tukumbuke watu wazima wengine uzoefu wao si msaada bali ni kigingi au kizuizi cha kufanya kazi ya Mungu. Wao huchuja mambo kupita kiasi, na imani yao inaenda na wanayoyaona zaidi ya wale wachanga wa imani.

Baadaye Petro alitembelea kanisa la Antiokia, na akafurahi alipoona watu wa mataifa wengi, akawatembelea majumbani mwao na kula nao, nao wakawaona ni wenzao. Ila Petro alighafilika tena, akaanza kuona aibu na woga mbele ya Wayahudi waliokuwa mafarisayo waliobadilika na kuwa Wakristo. Akajaribu kuepuka kufanya ushirika na Wakristo wasio Wayahudi. Tabia hii leo tunaita undumila kuwili, na wengi tumeanguka nayo, ila ni vyema kuwekana sawa.
Paulo aliposikia haya hakupendezwa na akamchukua Petro pembeni na kumwelezea kosa analofanya. Akamweleza hata yeye kama Myahudi, hatunzi yale mapokeo ya zamani ya Sheria za Musa kama kutoa kafara na mengineyo halfa za kutoa kafara (ceremonial laws) Sasa Kwa nini anataka kuwatwika watu wa mataifa walioongoka kuwa Wakristo na kongwa hilo. Mungu hatuokoi kwa sababu tunashika sheria hizo za Wayahudi, bali anatuokoa kwa kumwamini Yesu. Paulo ameandika kwa kina haya kwenye barua ya Wagalatia na Warumi, chukua muda kusoma barua hizo.

Alisema kama tunaamini kwamba matendo ya sheria ndiyo yatatufanya tuwe na uzima wa milele basi tumedanganyika. Hata tukiwa na matendo mazuri kiasi gani, hayawezi kutokoa. Ila hii haina maana tusishike sheria. Ila mahusiano na Mungu wetu ndiyo muhimu zaidi maana yatatufanya tuone sheria kuwa ndiyo inayoratibu mahusiano yetu na Mungu na wanadamu wenzetu. Kazi ya sheria ni kutuonyesha makosa, sawa na kioo. Mtu anapojiangalia kwenye kioo, hategemei kioo kumwondelea uchafu alionao, bali kioo kitamtambulisha kuwa kuna dosari au uchafu. Ni juu yake baada ya hapo kutafuta maji na sabuni ili kuondoa uchafu huo. Petro alimsikiliza Paulo na kuungama kosa lake, asitake kujificha.

Kutaka kupata wokovu kwa kutimiza mapokeo, na sherehe za kidini, ni kutoka katika mstari wa dini ya Kweli. Kuna sheria zile zinazohusu tabia zetu za Wakristo. Sheria hizo kama Amri Kumi, zitaendelea kudumu milele. Bali zingine kama kutoa dhabihu na kutahiriwa vilikuwa vya muda, vilikoma Yesu alipokufa msalabani.

*Tukimkaribia Mungu, ataweka neno kinywani mwetu kuzungumza kwa niaba yake, hata sifa kwa Jina Lake. Atatufundisha mkazo kutoka katika wimbo wa malaika, hata shukrani kwa Baba yetu wa mbinguni. Katika kila tendo la maisha, nuru na upendo wa Mwokozi anayeishi ndani vitafichuliwa. Shida za nje haziwezi kufikia maisha ambayo yanaishi kwa imani katika Mwana wa MUNGU.

------------------------------

Maswali: Kikao cha Yerusalemu kiliitwa kwa ajili gani? Kikao hiki cha mitume kiliamua nini na kuandika kwenye barua? Kikao hichi kilikuwaje msaada kwa injili kufika kwetu leo Afrika na kila mtu kuwa huru kuwa mshiriki wa kanisa la Kristo? Ni nani alikuwa anaamua katika kikao hiki? Kwa nini Paulo alimwonya Petro? Kwa nini Wakristo wa mataifa mengine walifurahi?

**SIKU YA 310.**
**(Novemba 5)**

# Paulo na Sila waimba gerezani.

**Matendo 16.**

Paulo akafika Debre na Listra kule Ulaya, na palikuwa na mwanafunzi muumini aitwaye Timotheo, mama yake alikuwa Myahudi aliyeamini, ila baba yake Mgiriki. Alishuhudiwa vyema na waumini wengine kwa sifa nzuri za tabia njema na kupenda mambo ya kiroho. Paulo akamwambia afuatane naye, akamtahiri, ili asiwakwaze Wayahudi. Huyu akawa mwana mpendwa wa Paulo katika Kristo. Wakipita katikati ya miji ile Paulo aliwapa barua iliyoandikwa na baraza la mitume, na watu wanaotakiwa kukamatwa. Makanisa yakatiwa nguvu katika ile imani.

Hesabu yao ikaongezeka siku hata siku. Wakapita Frigia, Galatia, na wakikatazwa na Roho wasihubiri Asia, au Bithinia. Wakapita Misia, wakaenda mpaka Troa. Wakati huu Luka 'tabibu mpendwa' alikuwa amejiunga nao. Huyu yawezekana alikuwa msaada kuwasaidia watu pia katika mambo ya afya. Wakiwa Troa, Paulo akapata maono usiku, ya mtu wa Makedonia huko Uyunani akiwa amesimama akimwambia "vuka uje kwetu Makedonia utusaidie." Basi wakapanga kwenda Makedonia Ulaya, wakijua Mungu amewaita kuhubiri habari njema.

Wakang'oa tanga na kufika Troa, na Samothrae, kisha Neopoli. Wakapita Filipi, mji mkuu wa Makedonia, mahali Warumi walihamia. Wakikaa pale siku kadha wa kadha, siku ya Sabato walitoka na kwenda kando ya mto ambapo walidhani pana mahali pa kusali, wakazungumza na wanawake waliokutana nao pale. Mwanamke mmoja aliitwa Lidia, mwuzaji wa mavazi ya zambarua, mwenyeji wa Thiatira mcha Mungu. Aliwasikiliza maana alikuwa ameufungua moyo wake kwa BWANA, na akataka ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo.

Lydia alibatizwa na kuwasihi mitume waje kwake akisema "kama mmeniona kuwa mwaminifu kwa BWANA, ingieni nyumbani mwangu mkae." Walipoona anawashurutisha, walijua alimaanisha kwa ule ukarimu wake kwao. Lydia alitaka kusikia zaidi Neno la uzima. Watu wengine husema njoo kwangu na wala hawana maana hiyo moyoni, bali wanataka ufikiri wanapenda watu na wanataka wageni, kumbe katika mioyo yao wanaomba useme "La." Hukaribisha watu kutimiza wajibu. Hili halitakuwa fungu letu, ndiyo ombi langu. Kukaribisha wageni hasa wanaotuletea habari za Mwenyezi Mungu ni baraka kubwa. Ni baraka kukaribisha wale wasio na mishahara kama wachungaji na maaskofu wa siku zile. Na wale wanaokaribishwa wasiwe mzigo kwa wenyeji wao, wasitake kutumikiwa wanapokaa wiki kadhaa kwenye nyumba fulani. Kitabu cha Shuhuda kwa Wachungaji na Watenda Kazi wa Injili, kimezungumzia sana kuhusu watumishi wanaoenda kutembelea watu wakitaka wale wenyeji wawafulie nguo zao, wawasanyie kuni, wawapikie vitu vitamutamu, na kazi zingine nyingi ambazo ni mzigo kwa hawa watu wasio na uwezo wa kihali au kimali. Kwenda kwenye uinjilisti si likizo au maburudisho fulani ambayo yanafanya

tuwape watu wengine shida wakati sisi tukijifurahisha. Kazi za mikono ni muhimu kwa kila mtu. Paulo alikuwa na bidii ya kazi ya kutengeneza mahema na kuuza ili kujikimu maisha, japo alikuwa na shahada ya udkatari wa theolojia. Lidia alikuwa yule mtu ambaye Paulo alimwona kwenye maono, akisema "Uje kwetu Makedonia." Walipokuwa wakienda kusali kijakazi mmoja aliyekuwa na pepo wa uaguzi, aliyewapatia bwana zake faida nyingi kwa kuagua au kuwaambia watu mambo yatakayotokea, yaani kubashiri. Huyu akawakuta wakina Paulo na kuwafuata kila mara akipiga kelele; "Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenye kuwahubiria njia ya wokovu." Hawakuwa na haja ya kulipia matangazo kwamba watu waje kwenye efoti, hawakuwa na haja ya kipeperushi kujitangaza, huyu kijakazi aliwafagilia njia! Alipofanya hivi siku nyingi, Paulo alisikitika na kufadhaika, maana walileta vurugu watu wasisikilize Maneno ya Mungu. Masikini huyu binti alikuwa chini ya nguvu za giza ambayo ni sawa na ugonjwa mzito, na mtume Paulo akamwonea huruma. Siku moja akifanya hayo, Paulo akageuka na kumkemea yule pepo aliye ndani ya yule msichana akisema "nakuamuru kwa Jina la Yesu Kristo, mtoke huyu." Pale pale yule pepo alimtoka.

Hata leo tutambue kwenda kwa wabashiri au wanajimu ni dhambi, Mungu Ndiye ajuaye yatakayotokea huko mbeleni. Wabashiri wako kwenye magazeti, njiani, na kila mahali. Wanatufuata watubashirie na kisha tuwalipe pesa. Ni dhambi kwenda kwa wabashiri, au wachawi. Hawa wanafanya kazi pamoja na ufalme wa giza. Wabashiri wanasema mengi ya kweli, kwa sababu Shetani ana uwezo kidogo wa kujua mambo zaidi ya sisi binadamu. Ila haya mambo anayoyajua hayatusaidii. Je hatupaswi kwenda kwa Mungu anayejua yote atubashirie mambo yetu, badala kwenda kwa Shetani? Hata hivyo kama unamjua Mungu wewe unajua yale yatakayowatokea wabashiri siku za mwisho kuliko wao. Na mambo mengine ya mbeleni tukiyajua hakika hayatatusaidia ila yatatutia hofu tu.

Wale waajiri wake, walichukia maana walimtumia walipotaka kupata mali, bila kujali kongwa la Ibilisi kwa msichana huyu. Walipoona tumaini la faida yao limewapotea, waliwakamata Paulo na Sila. Kisha wakawakokota mpaka sokoni mbele ya wakuu wa mji. Wakasema watu hawa Wayahudi wanachafua mji wetu. Wanatangaza hapa kwetu destruri zisizokuwa za halali kwetu kuzipokea, wala kuzifuata, maana sisi tu Warumi. Makutano wote wakawaendea mitume na wakawavua nguo kwa nguvu na kutoa amri wachapwe viboko.

Walipowapiga mapigo mengi kwa bakora, waliwafunga gerezani. Wakamwamuru mlinzi wa gereza awalinde sana, naye mlinzi akawatupa chumba cha ndani, na kuwafunga miguu na mkatale. Paulo na Sila hawakulalamika bali wakiwa na moyo wa shukurani, walimwomba Mungu usiku kucha, na kumsifu Mungu kwa nyimbo, huku wafungwa wengine wakiwasikiliza. Ghafla usiku wa manane kukatokea tetemeko kuu la nchi. Milango ya gereza ikatikisika, milango na vifungo vyote vikafunguka. Mlinzi wa gereza akaamka, na alipoona milango ya gereza imefunguka, alifuta upanga wake ili ajiue, maana askari Jela siku zile mfungwa akitoroka, aliuwawa. Paulo akapaza sauti kwa nguvu akimkataza yule askari, asijiue akasema, "usijidhuru kwa maana sisi sote tupo hapa."

Yule askari jela akataka taa iletwe, ili ahakikishe maana kulikuwa giza. Akarukia

ndani ya chumba cha mitume, akitetemeka kwa hofu, akawaangukia Paulo na Sila. Alikuwa amegundua mitume wana amani ya pekee, akajua wana kitu asichokuwa nacho. Akawatoa nje mitume na kuwauliza swali ambalo kwa kawaida askari jela hamwulizi mfungwa “Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka.” Wakamwambia “Mwamini BWANA Yesu wewe na nyumba yako nawe utaokoka.” Wakamwambia Neno la BWANA na yeye na watu wote waliomo nyumbani mwake. Askari huyu aliwakaribisha, usiku ule ule kwake, akawaosha majeraha yao ya mapigo.

Askari jela huyu akabatizwa, yeye na watu wake wote. Wakati uo huo, mitume walianza na vipigo wakaishia na kubatiza. Akawaandalia Paulo na Sila chakula, akafurahi sana, yeye na nyumba yake kwa kumwamini Mungu. Tunapomwamini Mungu, inatupa furaha kuliko kitu kingine duniani katika mioyo yetu, na maisha yetu hayatakuwa vile vile tena, tuna kitu ambacho tunaishi kwa ajili yake, tuna malengo bora. Hatutembei bila malengo tukisikitika kwamba tunapoteza muda. Kila anayemwamini Mungu na kumtii, ana uzima wa milele.

Wavulana na wasichana wengi michezoni au mashuleni ni rahisi kuwaumiza wengine kwa kuwakejeli, kuwacheka, kuwabagua au kuwanenea maneno ya kuumiza. Waweza kuwacheka chakula wanachokula, wazazi wao jinsi walivyo, kilema walicho nacho, umasiki wao au hata jinsi wanavyoonekana. Basi tujifunze kuosha na kufunga vidonda vya wale tunaowaumiza kwa kuwaomba msamaha. Dunia inahitaji waoshaji wa vidonda leo, iwe kwenye kanisa lako, shuleni kwako au familia yako, kuna hitaji la kuoshwa vidonda.

Kulipopambazuka, askari jela alipata maagizo kutoka kwa hakimu “waacheni watu hao waende zao.” Wakawaambia wale wafungwa wainjilisti waende zao kwa amani. Hakika watu wamepata mateso katika kulitangaza na kulileta Neno la Mungu. Paulo akasema imekuwaje waliwakamata bila kosa, na kuwaachia bila kuleta mashitaka nao ni Warumi. Watu wale hawakujua kwamba hawa ni Warumi. Viongozi walipojua, waliwasihi sana wakiomba msamaha wayaachie hapo, maana wangeingia kwenye matatizo. Wakawatoa nje ya mji wao na kuwaomba kwa adabu “tunawasihi mtoke mji wetu, tafadhali!” Hawakujikimbiza watoke hapo hapo, bali walikwenda kwa Lidia kwanza, kuwafariji ndugu na kisha wakatoka mjini mle.
Kweli Neno la Mungu litatuepusha na dhambi, japo dhambi pia inaweza kutufanya tuepuke Neno la Mungu

*Maombi yanahitajika Kila Siku Ili Kumpinga (kumsukuma) Shetani — Utakaso sio kazi ya nukta moja, saa moja au siku moja. Ni ukuaji endelevu katika neema. Hatujui hata siku moja mzozo wetu utakuwa na nguvu kiasi gani siku inayofuata. Shetani anaishi, na anafanya kazi kwa bidii, na kila siku tunahitaji kumlilia MUNGU kwa dhati ili kupata msaada na nguvu za kumpinga. Maadamu Shetani anatawala tutapaswa kutiisha ubinafsi daima, tutakuwa na usumbufu na mashambulizi ya kukabili, na hakuna mahali pa kusimama, hakuna hatua ambayo tunaweza kuifika na kusema tumeiwezea kikamilifu bila msaada Wake.
-------------------------

Maswali: Paulo alikutanaje na Mwana wake katika Kristo Timotheo? Paulo alipata ndoto ya kufika Makedoni akiwa wapi? Paulo aliwezaje kumfikia Lidia na wenzake kule Filipi? Lidia alikuwaje mbaraka kwa umishonari? Kwa nini si halali kumwacha mtu awe 'mgonjwa' au na pepo kama kijakazi, au kumtumia kuwa kitega uchumi? Elezea Paulo na Sila walipoingia gerezani nini kilitokea?

**SIKU YA 311.**
**(Novemba 6)**

# Watu waliopindua ulimwengu juu chini.

**Matendo 17.**



Wakapita Amfipoli, na Apolonia wakafika Thesalonike kwenye sinagogi la Wayahudi. Twajua Paulo aliandika barua zake za kwanza kwa washiriki wa Thesalonike kuwapa moyo, kuwashauri, na kuwafundisha mambo ya imani. Yawezekana hii ilikuwa barua yake ya kwanza. Paulo kama desturi yake akaingia pale na kuhojiana na Wayahudi, Maneno ya Maandiko kwa Sabato tatu akiyafunua mambo ya Yesu Kristo, aliyeahidiwa kwamba imempasa kuteswa na kufufuka katika wafu, na kwamba Yesu huyu Ndiye Masihi aliyeahidiwa. Wengine miongoni mwao wakaamini, na Wayunani pia walikuwa wengi sana. Na hata wanawake wengi walijiunga.

Wayahudi wakaona wivu na kujitwalia watu wa ovyo wahuni wasio na sifa njema, nao wakafanya ghasia mjini. Wakamwendea Yasoni na nyumba yake aliyekuwa muumini, wakamkamata. Baada ya kuwakosa wakina Paulo kwenye nyumba yake, wakasema "watu hawa walioupindua ulimwengu juu chini wamefika kwetu na Yasoni amewakaribisha, na wanatenda kinyume cha Kaisari mtawala wetu, wakisema yupo

mtawala mwingine aitwaye Yesu Kristo." Wakawapa wale waumini waliokutanika fadhaa, na wakamtoza Yasoni dhamana na kumwacha aende zake.

Ndugu wakawapeleka Paulo na Sila Beroya. Waberoya walikuwa watu waungwana kuliko wale wa Thesalonike, maana walilipokea Neno la Mungu kwa uelekevu wa moyo, wakiyachunguza Maandiko kila siku, wahakikishe kama yale waliyoambiwa ndivyo yalivyo, au watu wamejitungia yao tu. Basi watu wengi Wayunani wakaamini, na wanawake wa Kiyunani wasio wachache. Kweli mitume walipindua dunia juu chini, yaani walifanya mabadiliko duniani kwa kuwahubiria watu kuhusu Yesu. Je, wewe unapindua mtaa wako au mji wako juu chini? Je, unasoma Maandiko ya Mungu na kusali kila siku, ili nawe uupindue ulimwengu? Je ungeshitakiwa mahakamani kuwa u mkristo, watu wangepata ushahidi wa kutosha? Tujihadhari tusipinduliwe na mafundisho ya uongo.

Lakini Wayahudi wa Thesalonike walipopata habari kwamba Neno la Mungu linahubiriwa na Paulo, wakasafiri hata Beroya kwenda kuleta ghasia, na machafuko wakifadhaisha makutano. Ndugu wakampeleka Paulo pwani aende Athene, mji mkuu wa Uyunani ila Sila na Timotheo walibaki. Sila na Timotheo, wakaagizwa wasikawie kwenda Athene. Paulo akiwangojea, alitembea na kuona sanamu zimejaa tele, na roho yake ikachukizwa sana. Aliendა kwenye sinagogi na kuhojiana na Wayahudi wanaomcha Mungu wa mbinguni, na wale waliokutana naye sokoni kila siku. Wanafalsafa Waepikureo na Wastoiko, wenye ujuzi wakakutana nao wakipenda kujadili (debate).

Wengine wakasema mpuzi huyu anasema sema nini hapa, wengine wakasema "anaonekana anatangaza habari za miungu migeni, kwa maana anahubiri habari za Mtu aitwaye Yesu na ufufuo. Walipofikiria kuna haja ya kumsikilizika, walimshika na kumchukua Aeropago, nje ya mji kwenye mlima ambao waliuweka wakfu kwa mungu wao Mars. Wakamwambia Paulo, tuambie zaidi kuhusu elimu hii mpya unayoinena, kwa maana unaleta mambo mageni masikioni mwetu, tutapenda kujua, tuambie. Waathene wa Uyunani na wanafunzi wa vyuo vikuu waliokuja kusoma hapa walipenda sana kutumia muda wao kusimulia au kusikiliza mawazo au mambo mapya. Walijiona ni watu wenye maarifa mengi, na akili tele, wakajishughulisha kutoa mihadhara hapa.

Paulo akasimama katikati ya Aeropago kwenye kilima hiki na kusema "Enyi watu wa Athene, katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari mno mambo ya dini. Kwa kuwa nilipotembelea mji wenu, nimeona sanamu nyingi, madhabahu mbali mbali, na moja imeandika kwa maneno haya "KWA MUNGU ASIYEJULIKANA." Basi mimi nawahubirini habari Zake huyu Mungu Ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua. Mungu aliyeufanya ulimwengu, nchi, bahari, na vyote vilivyomo. Yeye ni BWANA wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mkono. Wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu chochote au hatengenezwi na mikono ya watu.

Ni Yeye Ndiye anatupa wote uzima, pumzi, na vyote. Naye Ndiye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, yaani Adamu, wakae juu ya uso wa nchi

yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu mwanzo na kutengeneza wapi wataishi; ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa papasa wakamwone. Japo Yeye hawi mbali na kila mmoja wetu. Mungu huyo sisi sote ni wazao Wake, kama watunga mashairi wenu walivyosema, kwa maana ndani Yake Yeye tunaishi, tunakwenda na kuwa na uhai. Kwa kuwa sisi ni wazao wa Mungu haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa dhahabu au fedha au jiwe, vitu vilivyochongwa kwa ustadi, na akili za wanadamu.

Zamani zile za ujinga ambazo hatukuelewa na tukamwabudu Mungu visivyo, Mungu alijifanya hazioni; ila sasa amejionyesha kwetu kwa njia ya Mwanawe Yesu Kristo na Maandiko matakatifu ambayo kila mtu anasoma, basi anatuagiza watu wote wa kila mahali tutubu. Maana ameweka siku ya hukumu kwa kila binadamu. Kwa ushahidi amemfufua Kristo katika wafu. Paulo alipoanza kuzungumzika kuhusu Yesu na ufufuo, wale wazee wa mji walifanya dhihaka, na kuingilia hotuba yake, na kumwuliza uhalisi wa ufufuo. Walikuwa si watu wabaya au wakatili wa kuua mtu, ila hawakuwa wasikivu kuhusiana na wokovu wao. Basi wengine walisema "njoo siku nyingine, tutakusikiliza tena katika habari hiyo ya ufufuo." Paulo alihubiri kisa chote cha msalaba na alitoka akawaacha, ila baadhi ya watu wakashikamana naye na wakaamini, kama Dionisio Mwareopago na mwanamke aitwaye Damari na wengine.

Hata leo kuna wengi waonekana si watu wabaya, ila hawako tayari kuamua mambo ya wokovu wao. Paulo alisikitika, akaona kwamba pengine safari ijayo hatatumia falsafa sana kama Wayunani akionyesha kwamba yeye ni msomi, na hivyo kujipotezea muda. Kazi hiyo ya kujadili falsafa waliyoifanya wakina Socrates, Plato na Socrates na wengine haifai kwa Mkristo kuifanya kamwe. Aliazimia atamhubiri Kristo moja kwa moja, maana matunda ya Athene ya watu kuamua kumfuata Kristo yalikuwa madogo.

Siku hizi zimeibuka nadharia nyingi sana ambazo ni kinyume na Mungu wa mbinguni. Nadharia za miungu wengi kama patheisimu na zile zinazosema Mungu si nafsi hai. Yabidi tuyarudie Maandiko kujua yanasema nini.

Kuhusu Kristo imeandikwa: "Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu." Yohana 1: 4. Yeye Ndiye Chemchemi ya uzima. Utii Kwake ni nguvu inayotoa uhai unaofurahisha moyo. Maarifa ya Mungu kama yanavyofunuliwa katika Kristo ni maarifa ambayo wote ambao wameokolewa lazima wawe nayo. Neno la Mungu ndiyo ulinzi wetu, ikiwa hawaendi kwa sheria au ushuhuda basi hamna nuru hapo.

Uwanja ambao ndani yake Shetani aliwaongoza wazazi wetu wa kwanza ndio uo huo ambao anawaongoza watu leo kuuingia. Anaujaza ulimwengu na hadithi za kubuni za kupendeza. Kwa kila hila iliyo chini ya mamlaka yake anajitahidi kuwazuia watu kupata maarifa ya Mungu ambayo ni wokovu. Yeye aliye na ufahamu wa Mungu na Neno Lake ana imani thabiti katika Uungu unaozungumzwa katika Maandiko Matakatifu. Haipimi Biblia kwa mawazo ya mwanadamu ya kisayansi. Bali analeta mawazo haya kwenye kipimo chenye kiwango kisicho na makosa. Anafahamu

kwamba Neno la Mungu ni Kweli, na Ukweli hauwezi kujipinga kamwe; Chochote katika mafundisho ya kile kinachoitwa sayansi kinachopingana na Ukweli wa mafunuo ya Mungu ni kazi ya mwanadamu kubahatisha tu.

Kwa wenye hekima hasa, utafiti wa kisayansi hufungua uwanja mpana wa fikira na taarifa. Njia za Mungu kama zinavyofunuliwa katika ulimwengu wa asili na katika namna anavyoshughulika na mwanadamu hubeba hazina ambayo kutoka humo kila mwanafunzi katika shule ya Kristo anaweza kuchota. Ushahidi wa kweli wa Mungu aliye Hai haupo katika nadharia tu; bali pia katika usadikisho ambao Mungu ameuandika katika mioyo yetu, ukiangazwa na kuelezewa na Neno Lake. Ni katika uweza ulio hai wa kazi Zake alizoziumba, na kuonekana kwa jicho ambalo Roho Mtakatifu ameliangazia.

*Maombi ya Kila Siku yajumuishe Mahitaji ya Kimwili na Kiroho— Maombi ya mkate wa kila siku yanajumuisha sio tu chakula cha kutegemeza mwili, lakini mkate wa kiroho ambao utarutubisha na kulisha roho hata kwenye uzima wa milele. Yesu anatuagiza, "Msikifanyie kazi chakula chenye kuharibika, bali kile kidumucho hata uzima wa milele."Yohana 6:27. Anasema, "Mimi Ndimi mkate hai uliyoshuka kutoka mbinguni. Mtu yeyote akila mkate Huu, ataishi milele." Mstari wa 51. Mwokozi wetu ni mkate wa uzima, na ni kwa kutazama upendo Wake, kwa kuupokea rohoni, ndio tunakula mkate ulioshuka kutoka mbinguni.
-----------------------------

Maswali: Kwa nini watu wa ovyo walienda kwa Yasoni? Mtu anaweza kuwa mtu wa ovyo kwa namna gani? Watu gani waliamini kule Athene? Kwa nini kuwa mtu mzuri tu bila kuamua kumfuata Mungu ni kuchagua kuwa mtu mbaya hatimaye? Twawezaje kuwa waungwana leo kama Waberoya? Mjadala wa Falsafa na Wayunani ulimsaidiaje Paulo? Je, wewe umeupindua ulimwengu wako juu chini kwa kumshuhudia Kristo? Kwa nini watu husema nchi za magharibi zinaanzia Uyunani? Ni nadharia gani ambazo umeshawahi kuzisikia ambazo zinapingana na mafunuo ya Mungu? Je, leo wewe unaupindua ulimwengu juu chini kwako kwa kuwaambia watu habari njema?

**SIKU YA 312.**
**(Novemba 7)**

# Akila, Prisila, na Apolo.

**Matendo 18**

Paulo akatoka Athene, akafika Korintho, na kule alimwona Myahudi aitwaye Akila, na mke wake Prisila, hawa walitoka Ponto Italia, kwa sababu Kaisari Claudio mtawala wa Rumi aliamuru Wayahudi wote watoke huko. Paulo akafika hapa ahubiri injili. Akila na mkewe walikuwa na biashara ya kushona mahema nao wakamkaribisha Paulo akae kwao. Wakamwajiri atengeneze mahema nao. Paulo akaenda kwenye sinagogi kila Sabato na kutoa hoja au kuhubiri akijaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani.

Sila na Timotheo wakafika toka Makedoni, kisha Paulo akaenda nao kwenye sinagogi akisukumwa na lile Neno la kumshuhudia Yesu Masihi aliyefufuka katika wafu. Walipopingana naye na kumtukana Mungu, akakung'uta mavazi yake akawaambia, "Damu yenu iwe juu ya vichwa vyenu, kwa kutoamini kwenu, dhamira yangu ni safi, nitakwenda kwa mataifa." Alitoka pale na kwenda kwa nyumba ya Tito Yusto mcha Mungu Ambaye nyumba Yake ilikuwa inapakana na sinagogi. Huyu alimwamini BWANA Yeye na nyumba Yake. Naye Krispo mkuu wa sinagogi alipomwamimi BWANA Wakorintho wengi waliamini wakabatizwa.

BWANA alimjia Paulo kwa maono usiku akamwambia "Usiogope kunena habari njema, kwa kuwa Mimi Nipo pamoja nawe, wala hapana mtu atakayekushambulia au kukudhuru, kwa maana Mimi nina watu wengi katika mji huu" Paulo akakaa kule Korintho mwaka na nusu akifundisha Neno la Mungu. Paulo anasema sisi binadamu ni vyungu vya udongo thamani yetu ni ndogo, ila tumebeba hazina kubwa yaani injili ndani ya hivi vyungu. Sisi tu vyombo vya udongo, Upendo wa Yesu ni motisha kubwa ya kutufanya tusifanye dhambi.

Galio alipokuwa gavana wa Akaya, Wayahudi wasioamini wakamwinukia Paulo kwa njia moja na kumleta mbele ya kiti cha hukumu wakisema "mtu huyu huwavuta watu ili wamwambudu Mungu kinyume cha sheria. Paulo akafungua mdomo, anene ila Galio hakutaka kujiingiza katika magomvi ya dini, akawafukuza wasimghasi akisema "kama ni mambo yahusuyo dhuluma, hila mbaya au uhalifu ingekuwa haki mimi kuyasikiliza na kuchukua hatua, bali ikiwa ni hoja juu ya sheria na dini zenu Wayahudi, ninyi wenyewe yaangalieni hayo , maana mimi sitaki kuwa mwamuzi wa mambo hayo."

Alipowafukuza waondoke, mahakamani, Wayahudi wote wakamshika Sosthene mkuu wa sinagogi na kumpiga mbele ya kiti cha hukumu, Galio hakuonyesha kujali yale wanayoyafanya. Japo wengi walichukia wahubiri na kazi ya injili, Paulo alijua hana haja ya kuhofu kwani Mungu alizungumza naye usiku mmoja, kwamba hakuna madhara yatampata.

Paulo alikaa pale kwa siku nyingi, kisha akaaga ndugu na kwenda Shamu, na Akila na Prisila wakaenda pamoja naye. Paulo akanyoa nywele zake kule Kenkrea maana alikuwa ameweka nadhiri ya kujikabidhi upya kwa Mungu. Kwa kawaida waliweka nywele hizi na kwenda nazo Yerusalemu kwenye madhabahu ambapo nywele hizi zingechomwa na angetoa sadaka pale. Wakafika Efeso keshoye na akaingia kwenye sinagogi akihojiana na Wayahudi. Walipomtaka akae, nao, aliwaambia atarudi tena, Mungu akimjalia. Akashuka Kaisaria na kusalimu kanisa. Kisha akaenda Antiokia, na akisha kaa siku kadhaa, akapita Galatia, na Frigia mji kwa mji akiwatia moyo na kuwaimarisha washiriki, kwa kuwathibithishia Ukweli wa Maneno ya Mungu.

Watu wa Galatia walikuwa na moyo wa ukarimu na wakampokea Paulo vizuri kama 'Malaika wa Mungu, au Yesu Mwenyewe.' Paulo mwenyewe anasema, walikuwa tayari hata kutoa macho yao wampe kama angeyahitaji, alimradi tu injili iende mbele. Ila watu wa Galatia walighafilishwa na walimu Wayahudi waliowapotosha kwamba wapaswa kuwa Wayahudi na kushika mapokeo ya Wayahudi ili waokolewe. Hapo ndipo Paulo aliamua kuandika barua "hivi ni nani aliyewaloga mkaacha niliyowafundisha na kushika maneno mengine yanayowafunga. Ninyi ni huru katika Kristo sheria za kutahiriwa na zingine zimepitwa na wakati"

Hapa walimkuta Myahudi mmoja aitwaye Apolo, mzaliwa wa Iskanderia Misri. Huyu alikuwa mtu wa mwenye elimu kubwa, na mzungumzaji hodari wa Maandiko. Huyu alikuwa amefundishwa njia ya Bwana na Roho yake ilimwaka. Alifundisha watu kwa kunena kwa ujasiri katika Sinagogi, ila alijua ubatizo wa Yohana tu, bali hakujua kuhusu Masihi aliyezaliwa, na kuishi, na hatimaye kufa na kufufuka. Akila na Prisila walipomsikia walimchukua kwao wakamweleza kwa kina mpango wa Mungu wa wokovu, kupitia Yesu Kristo Masihi. Apolo akaamua kutoka Asia ndogo na kwenda Uyunani. Kabla ya kwenda waumini walimwandikia barua ya utambulisho, ili waumini na wanafunzi wa Kristo wa kule wamkaribishe kwa moyo wote.

Alipofika kule aliwasaidia sana wale waliokwisha kuamini kwa neema ya Mungu, kwa maana aliwaeleza vizuri kuliko wengine na kwa undani walielewa kisa cha wokovu na injili. Akaonyesha kwa Maneno ya Maandiko kuwa Yesu ni Kristo. Paulo anamtaja Apolo kama shujaa mkubwa, na baadaye watu walipoanza kusema mimi ni wa Apolo au Paulo kutokana na yupi aliwasaidia kuwaleta kwenye imani, Paulo alisema kwamba Apolo au yeye hawakufa kwa ajili yao. Ni Yesu tu, hakuna mtu wa mtu fulani, kwani sote ni wa Mungu! Wakristo wote ni viungo vya mwili wa Kristo, Yesu ndiyo kichwa. Mwili huu umegundishwa pamoja kwa nguvu za Roho Mtakatifu na Upendo wa Mungu. Tunapaswa kuwa ndani ya Yesu, na si kujichomeka kwa watu.

Kanisa la Korintho lilikuwa moja wapo ya makanisa ya wakati ule. Walikuwa na bandari iliyopeleka merikebu nchi mbali mbali, ulikuwa mji wenye maendeleo ya kisasa siku zile. Waumini wengine walighafilishwa na tabia potofu na uhalifu wa mji ule. Hii ndiyo sababu ya Paulo kuandika barua kama nne hivi alipotoka Korintho kuweka mambo sawa. Mojawapo ya vitu alivyoandika ni upendo kwamba ni kitu muhimu sana.

*Tunampokea Kristo kupitia Neno Lake, na Roho Mtakatifu anatolewa ili kulifungua Neno la MUNGU katika ufahamu wetu, na kuleta Kweli Zake mioyoni mwetu. Tunapaswa kuomba siku baada ya siku kwamba tunaposoma Neno lake, MUNGU atume Roho Wake ili kutufunulia Ukweli ambao utaimarisha roho zetu kwa hitaji la siku.

---------------------------

Maswali: Paulo alisaidiwaje na Prisila na Akila? Galio alimwokoaje Paulo? Apolo alipungua mafundisho gani bila yeyé mwenyewe kujua? Damu yenu iwe kwenye vichwa vyenu, ina maana gani? Paulo alipata maono gani ya kufariji akiwa Korintho? Kuna ubaya gani kujipajichika kwa mtu fulani badala ya kujikabidhi kwa Yesu? Paulo alianzisha makanisa na kuyatembelea akisaidia kwa kuandika barua kama mlezi na kuhimiza washiriki watoe Zaka na Sadaka, Je walitumia Zaka na sadaka kwa jambo gani? (Warumi 15:26 na 2 Wakorintho 8:1-4).

**SIKU YA 313.**
**(Novemba 8)**

# Vitabu vya uovu vyachomwa moto.

**Matendo 19.**

Apolo alipokuwa akihubiri Korintho, Paulo alipita Asia ndogo kwa mguu na kufika Efeso kama alivyoahidi, na alikutana na waumini wapya. Hawa waliitwa wanafunzi wa Yesu. Paulo aliwauliza kama walipokea Roho Mtakatifu walipoamini? Wakamjibu La! wala hatujawahi kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu. Alipowauliza, basi mlibatizwa kwa ubatizo gani, wakasema kwa ubatizo wa Yohana. Paulo akawaambia, Yohana alibatiza ubatizo wa toba, kuungama dhambi, ila aliwaambia watu watazame, Masihi anayekuja nyuma yake, yaani Yesu. Waliposikia mahubiri haya, walibatizwa kwa Jina la BWANA Yesu. Paulo alipoweka mikono yake juu yao, walipokea Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri, na jumla yao walikuwa 12. Tuna somo la kujifunza toka kwa watu hawa, wakisikia mafundisho ya Yesu, wapo tayari kusahihisha njia yao ya mapokeo, na kufuata Kweli.

Paulo akaingia katika Sinagogi akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu akihojiana na watu na kuwavuta, katika mambo ya ufalme wa Mungu. Bali wengine walikataa kuamini, wakitukana yale mafundisho mbele ya mkutano. Paulo akaondoka, baada ya kuwatenga waumini wapya, yaani wanafunzi wa Yesu. Akahojiana na watu katika nyumba ya muumini Tirano. Mambo yakaendelea vile kwa miaka miwili, akimaliza na kundi moja alichukua jingine na kuendelea kuwafundisha, mpaka wote waliokaa Asia wakapata nafasi ya kusikia Neno, Wayahudi na Wayunani.

Mungu akatenda miujiza na ishara zisizo za kawaida, kupitia mikono ya Paulo, hata wagonjwa wakaletewa leso na nguo zilizotoka mwilini mwake na magonjwa yao yakaondoka, na pepo wachafu wakawatoka. Wakati huu walitokea Wayahudi wenye pepo wanaotembea huku na kule wakidai kwamba wana nguvu za kuponya watu na kutoa pepo kwa njia za uchawi. Hawa walikuwa wana saba wa mtu kuhani aliyeitwa Skewa, nao walitumia Jina la Yesu kama ni hirizi au uchawi fulani, wakisema "Nawaapisha kwa Yesu yule anayehubiriwa na Paulo mtoke mtu huyu." Yule pepo mchafu aliwajibu wale vijana wanaochezea mambo matakatifu japo walijua fika maana baba yao alikuwa mchungaji "Yesu namjua na Paulo namfahamu, lakini nyinyi ni nani?" Na yule mtu aliyepagawa na pepo mchafu akawarukia wawili kati yao, akawashinda nguvu na kuwajeruhi. Nao wote saba wakatimua mbio, katika nyumba ile, wakiwa uchi na majeraha.

Habari hii ikajulikana na Wayahudi na Wayunani kote, na Jina la BWANA Yesu likatukuzwa, na wengi katika wale walioamini wakaja wakiungama matendo yao ya kushughulika na nguvu za giza na uchawi. Vijana hawa hawakusahau upuuzi waliofanya, na wakajua kwamba Jina la Yesu si la kufanyia utani. Hebu Mungu atusaidie tusiwe watoto au vijana wapuuzi tunaochezea mambo ya Mungu. Yapasa

tujue Jina la Yesu lina nguvu zote, ila linapaswa kutumiwa kwa kicho na kwa dhati, kwa wale wanaompenda Yesu ili kutoa mapepo au kutatua shida. Wengi kati ya hao waliotumia mambo ya Uganga wakakusanya vitabu vyao, wakavichoma moto mbele ya watu wote, wakafanya hesabu ya thamani yake ikapata fedha 50,000, hii ni sawa na dola milioni tatu leo. Neno la BWANA likazidi kushinda nguvu. Vitabu hivi ni vingi mno, hasa ukifikiria, kuwa ulikuwa wakati ambao hakuna mashine ya chapa na watu walinakili kwa mkono maandishi yote.

Hata leo vitabu vya uchawi vipo vingi zaidi, watoto wajihadhari na kusoma vitabu vyovyote viovu. Vitabu vya Harry poter, wicca, uchawi mweusi na vinginevyo. Kuna vitabu vingi vya giza, twabidi tuwe waangalifu sana kuchagua vile vya nuru. Vitabu vya tamthiliya vya mapenzi (romantic novels) na ujasusi vinapaswa kuepukwa. Je, unajua vitabu vya giza ni vipi? Waweza kuviorodhesha? Siku zile kulikuwa hakuna filamu, mikanda ya video, kompyuta, runinga au radio. Leo tuna vitu hivi, Je Waweza kusema vipindi gani vya radio, simu, au runinga vina uovu ambacho hupaswi kuvisikiliza? Je unayajua matangazo ya biashara unayopasa kuyaepuka? Kuna vitu vingine vinaonekana kama havina ubaya bali matunda na mvuto wake yameangusha wengi hivyo ni moto wa kuotea mbali. Vingine ni vya kukupotezea muda ili upoteze kulenga shabaha yako na kupata Mbingu, na badala yake ujikute umeangukia Jehanamu.

Mambo kama kucheza karata, au bao yamefuga uvivu mwingi, yameleta uraibu na kisha Neno la Mungu linapinga uvivu. Mbali na imani yetu kwa Mwenyezi Mungu, kazi ndiyo jambo linalofuatia kwa umuhimu. Twasoma miaka 30 Yesu alikaa kwao akifanya kazi ya useremela kwa mikono yake, na kisha alihubiri kwa miaka 3 na nusu tu. Bidii ya kazi ni jambo muhimu kutukinga na majaribu mengi pia. Kuchoma vitabu viovu vya kichawi kulipokwisha, Paulo akaazimu rohoni mwake kwenda Makedonia, Akaya na kisha aende Yerusalemu akitaka kuuona Rumi mji mkuu wa dunia yote siku zile kisha aende Hispania. Nia kuu, apeleke habari njema ya Yesu Kristo Masihi aliyefufuka katika wafu. Akatuma ujumbe Timotheo na Erasto, waje wamsaidie.

*Katika kutufundisha kuomba kila siku kile tunachohitaji—baraka za kimwili na za kiroho—MUNGU ana kusudi la kutimiza kwa manufaa yetu. Angependa tutambue utegemezi wetu juu ya utunzaji Wake wa kila mara, kwa kuwa anatafuta kutuvuta katika ushirika na Yeye Mwenyewe. Katika mawasiliano na ushirika huu na Kristo, kwa njia ya maombi na kujifunza zile Kweli kuu na za thamani za Neno Lake, kama roho zenye njaa tutalishwa; kama wale walio na kiu, tutaburudishwa kwenye chemchemi ya uzima.

---------------------------

Maswali: Kwa nini walichoma vitabu vile wasiviuze na kusaidia mali hiyo kueneza injili? Je vitabu gani unafikiri vyahitaji 'kuchomwa' au kutosomwa kamwe, katika ulimwengu wetu wa leo? Je, vipindi gani vya runinga au kompyuta hatuhitaji kuweka nyuso zetu huko? Kwa nini kuwa mtoto wa mchungaji au mtenda kazi wa kanisa si kibali cha kukana uovu?

**SIKU YA 314.**
**(Novemba 9)**

# Efeso na mungu wao wa kike aitwaye Artemi.

**Matendo 19**



Paulo alikaa Efeso miaka miwili. Waefeso walikuwa na hekalu kubwa la thamani kubwa, wakiweka vinyago mule na kuviabudu. Waefeso walipenda vinyago vyao vya mungu mke Dayana vilivyotengenezwa na wafua shaba na ambavyo waliviabudu. Hata leo mahali pengi hapa kwetu Afrika watu wametegeneza vitu fulani wanavyoviabudu. Wengine waweza kuabudu miti fulani au mambo fulani, badala ya mwenyezi Mungu. Watu wengi wamefanya biashara kwenye vitu vya imani wakijua watu watanunua. Na pale ambapo biashara yao inapoonekana kuzama kwa ajili watu wamegundua uongo au ulaghai wa sanamu zisizookoa, wanakasirikika na kutaka kuulinda ule ulaghai wao.

Watu wengi hudanganywa kuweka imani au matumaini yao kwenye sanamu, ambazo haziwasaidii kitu. Watu wengine wametumiwa vitambaa, miti na vitu fulani hata wale ambao ni Wakristo na kuambiwa watumie vitu hivi kama hirizi ya kufanikisha maisha yao. Hawa wameambiwa wavinunue hivi na vitawasaidia kuwa matajiri. Vitu hivi kwao vimekuwa vya muhimu kwenye ibada zao ili maombi yao yajibiwe, kuliko hata Mungu. Ibada za namna hii zinaweza kufanana na mambo ya ushirikina au uchawi. Watu wengi siku hizi wanaweza wasiwe na miungu ya namna hii bali vitu, mali, maoni, mitazamo, mahusiano, teknolojia au falsafa kama uibukaji vimekuwa miungu ya wengi.

Wakati huo ikatokea ghasia kubwa katika njia ile, mtu mmoja mfua fedha kule Efeso kwa jina Demetrio, huyu alikuwa akifanya vihekalu vya fedha vya Artemi Mungu wa kike wa Efeso au kwa jina jingine 'mungu' huyu aliitwa Dayana. Biashara yake ya kutengeneza hivi vihekalu ilienda mrama kwani watu walianza kumwamini Mungu wa Kweli wa Ibrahimu, aliyeumba mbingu, nchi, bahari na vitu vyote. Alipokosa soko

la miungu aliyoitengeneza alikasirika maana yeye na mafundi wengine walipata faida nyingi kwa kuuza miungu yake hiyo.

Akakusanya watu wanaohusika na ustadi ule, na kuwajaza maneno yake ya uwongo akisema "enyi wanaume, mnajua uchumi wetu hutokana na kazi hii, na katika Asia yote watu wananunua bidhaa hii kwetu. Sasa huyu Paulo amekuja hapa Efeso na Asia yote na kushawishi watu kugeuza nia zao na wote wanamfuata. Akasema ya kwamba hizo zinazofanywa kwa mikono siyo miungu ya kweli ya kutoka mbinguni na kwamba Artemi mungu wetu wa kike si Mungu. Watu wote sasa wanamwamini, biashara yetu na utalii itaanguka na kudharauliwa. Na hata hekalu la mungu mke aliye mkuu, Artemi atahesabiwa si kitu, na kuondolewa utufuku wake, ambaye Asia na ulimwengu wote humwabudu." Waliposikia haya walijaa ghadhabu, wakapiga kelele wakisema "Artemi wa Waefeso ni mkuu."

Mji wote ukajaa ghasia, wakaingia mahali pa ukumbi wa michezo kwa nia moja na kumkamata Gayo na Aristariko, watu wa Makedonia waumini na watenda kazi na Paulo. Paulo alipotaka kuingia kati ya watu aongee nao, waumini au wanafunzi wa Yesu hawakumwacha aingie wakijua atakuwa hatarini kuuwawa. Rafiki zake katika Kristo wakamtumia ujumbe wakisema asijipeleke kwenye jumba la michezo. Watu walikuwa na fujo, wengine wakisema hili na wengine lile, na wengi kati yao hakuwajua sababu ya kukusanyika kwao pamoja au kwa nini walikuwa wakipiga makelele, bali walifuata mkumbo tu. Je, wewe leo unafuata mkumbo wa watu, wakati hujui kichoendelea, bali unashabikia mambo tu, hili ni kosa, lazima uwe na msimamo, ukijua wewe ni nani, na upo hapa duniani kwaajili gani.

Jambo hili latokea siku hizi sana, wengi hawajui kwamba ni wakati wa kuwa karibu na Mwenyezi Mungu, na wakisikia wengine wanampinga Mungu wanaingilia kwa kuzomea zomea au kupayuka payuka, wasijue wanachokisema alimradi wako kwenye kadamnasi ya wengine. Twahitaji kujihoji kibinafsi, na si kufuata wanapoenda watu wengi, au penye mikumbo. Katika ufalme wa Mungu mara nyingi watu wengi wanaelekea njia ya uovu na wachache njia ya uzima. Msemo wengi wape, si sahihi sana tuendapo mbinguni. Ukikutana na watu wa namna hii, chunguza kwa makini kama yale wanayosema ni ya Kweli. Je, kinafuatana na Maandiko, kabla ya kujiingiza?

Basi wakiendelea kupayuka wasijue sababu ya kukusanyika kwao pamoja, wakamtoa Iskanda katika mkutano, Wayahudi wakamweka mbele ya watu. Isakanda akawapungia mkono, akitaka kutoa hoja ya kujitetea, ila walipojua kwamba yeye ni Myahudi walipiga kelele wote pia kwa sauti moja kwa masaa mawili wakisema "mungu wa kike Artemi wa Waefeso ni mkuu." Watu hawa walitumia nguvu nyingi kuzomea masaa yote haya mawili, ingelikuwa bora kama wangelitumia muda huo kufanya yale yatakayoleta manufaa. Maneno yao yakawa kama pambio hivi, walipozidi kuyarudia rudia, yalibadilisha hisia zao na kuwapandisha mori bila wenyewe kugundua.

Karani wa mahakama au mji kwa hekima aliwatuliza, na kuwaambia "Enyi watu wanaume wa Efeso ni mtu gani asiyejua ya kuwa mji wa Efeso ni mtunzaji wa

hekalu la Artemi, aliye mkuu na wa kitu kile kilichoanguka kutoka mbinguni?" Akawaambia mambo hayo ya mungu wao hayawezi kukanushwa, hivyo imewapasa kutulia, wasifanye maamuzi ya haraka haraka kwa mori au hisia tu. Akawaambia wahubiri hawa hawakuiba au kufanya uhalifu wowote wa vitu vya hekalu letu, toka walipoletwa 'hawajamtukana mungu mke wetu'.

Akawaamba ikiwa Demetrio fundi wa fedha na mafundi wenzake wana neno juu ya mtu, kuna baraza na sheria, na mahakimu, hebu apitie mchakato huo na kuleta mashitaka; ila mkianza kutafuta maneno mengine, na kuleta ghasia au ukorofi, yataibuka mambo mengine katika kusanyiko lililo halali. Tutajiletea hatari ya kushitakiwa na sheria ya Kirumi kwa matata haya ya leo, ambayo hayana sababu, nasi hatutaweza kutoa udhuru kwa mkutano huu kwa ghasia hii. Alipokwisha kusema vile aliuvunja mkutano na watu wakaenda makwao .


*Omba Kila Siku kwa ajili ya Baraka Inayoletwa na Sabato—Wote wanaoichukulia Sabato kama ishara kati yao na MUNGU, wakionyesha kwamba Yeye Ndiye MUNGU anayewatakasa, watawakilisha kanuni za serikali Yake. Wataleta katika utendaji wao wa kila siku sheria za ufalme Wake. Itakuwa ombi lao la kila siku kwamba utakaso wa Sabato uwe juu yao. Kila siku watakuwa na ushirika wa Kristo na wataonyesha ukamilifu wa tabia Yake. Kila siku nuru yao itawaangazia wengine kwa matendo mema.
----------------------------

Maswali: Demetrio aliwachocheaje watu mpaka wakafanya maandamano na fujo? Karani wa mji aliwatulizaje mafundi wa fedha? Kwa nini ni rahisi binadamu kupayuka payuka wasijue kinachoendelea kama wale wale watu wa mji wa Efeso?

**SIKU YA 315.**
**(Novemba 10)**

# Paulo awaaga waumini.

**Matendo 20**



Kishindo kilipokoma Paulo akawaaga waumini na akawaonya na kuwapa maneno ya kuwatia moyo, naye akaondoka zake kwenda Makedonia, akiisha kupita pande zile na kuwafariji kwa maneno mengi aliende mpaka Uyunani. Alikaa pale miezi mitatu, na Wayahudi wakamfanyia vituko wakitaka kumwua, alipotaka kwenda Shamu kwa njia ya bahari. Basi akaazimu kurejea kwa njia ya Makedonia, alifuatana na Sosparto Mberoya, Aristarko, Sekundo, wa Thesalonike, Gayo wa Derbe, Timotheo, na Tikiko na Trofirmo watu wa Asia. Hawa walimtangulia na kufika Troa.

Ilikuwa wakati wa pasaka, wakila mikate isiyochachwa kama maagizo waliyopewa walipotoka Misri, kwamba wale mikate isiyotiwa chachu, kuonyesha mwili wa Kristo hauna chachu. Wakatoka Filipo, wakafika Troa. Ilipofika siku ya kwanza ya juma waliumega mkate yaani sakramenti ya meza ya BWANA. Paulo akahubiri, akiazimia kuondoka keshoye, akafululiza kuhubiri mpaka usiku wa manane. Wakiwa ghorofani, taa zilikuwa nyingi za utambi na mishumaa, na kijana mmoja wa miaka

15 alitwaye Eutiko, alikuwa ameketi dirishani akalemewa na usingizi.

Alijaribu kufungua macho tena na tena lakini akashindwa. Saa za kawaida za watoto kulala zilikuwa zimepita. Paulo alipoendelea sana kuhubiri akazidiwa na usingizi wake, akapoteza umakini, akaanguka toka gorofa ya tatu, akainuliwa akiwa amekwisha kufa. Watu wakaanza kupiga mayowe kwa hofu, wakijua amekufa. Paulo akashuka ghorofani, akamkumbatia mwili wake, akasema "Msifanye ghasia maana uzima wake ungalimo ndani yake." Akapanda tena juu na kuendelea na ibada, akamega mkate na akala, na akaendelea kuongea nao, hata alfariji, ndipo akaenda zake. Wakamleta kijana Eutiko, yu mzima, amefufuka, wakafarijika faraja kubwa sana. Kuna vijana wengi kama Eutiko wanalala kanisani japo wana nia ya kusikia, hebu hawa watiwe moyo kwa njia fulani na kutafutiwa vitu vya kufanya kanisani, na pia mahubiri yasiwe marefu sana, isipokuwa Roho wa Mungu ameruhusu!

Kisa hiki kisikufanye ulale kanisani, kwani hata ni mtoto wapaswa kusikiliza mhubiri anachozungumza. Eutiko alilala kwa sababu ilikuwa usiku wa manane, watu walijaa, hamna pa kukaa, na alipenda kusikiliza, ila saa zilikuwa zimeenda. Kanisa si mahali pa kulala kama upo nyumba ya wagen, la! ni pahali pa ibada japo tutatoa udhuru hapa maana Paulo alikuwa akiaga wasimwone tena hivyo walijikaza wasikie kwa moyo mausia yake ya mwisho ya injili. Tabibu Luka akatangulia na wengine kwenda Aso, kumpata Paulo kule, aliyekuwa akitembea kwa miguu. Paulo hakulala, baada ya kumfufua Eutiko aliendelea kuhubiri mpaka asubuhi, na kuanza safari ya kilomita 30 hivi kwa miguu. Kweli huyu alikuwa shujaa wa kazi ya Mungu.

Walipofika Aso Paulo alipakia chombo wakaenda Kio, Samo, Trogilio, kisha Mileto. Paulo alitaka awahi Yerusalemu kupitia Efeso, ili awe kule wakati wa Pentekoste, yaani maadhimisho ya siku 50 baada ya Yesu kufufuka na kupaa Mbinguni. Pale Mileto Paulo alituma wazee wa makanisa ya Efeso waitwe. Wazee wa makanisa waliwekwa kusimamia makanisa mapya mara tu yalipoanza. Akawaambia wazee hawa "ninyi wenyewe mnajua tangu siku ya kwanza nilipokanyaga Asia jinsi nilivyokuwa kwenu wakati wote. Nilimtumikia BWANA kwa unyenyekevu wote na kwa machozi. Mnayajua majaribu yaliyonipata kwa ajili ya hila za Wayahudi.
Sikujiepusha katika kuwatangazia neno lolote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha wazi wazi, nyumbani mwenu nikiwashuhudia Wayunani na Wayahudi, bila ubaguzi kwamba wanapasa kutubu, na kumwamini BWANA wetu Yesu Kristo, basi angalieni sasa nakwenda, Yerusalemu kwa kumtii Roho Mtakatifu, nisiyajue mambo yatakayonikuta huko. Kile kidogo nachojua, ni kwamba Roho Mtakatifu, amenionyesha kwa njia moja au nyingine kwamba vifungo na dhiki vyaningoja. Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu, kinachojalisha ni kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa BWANA Yesu.

Nataka mjue kwamba mmekuwa wa thamani kwangu toka nilipoanza kuwahubiria injili. Naona kwamba nikienda huko, hamtaniona uso wangu tena; kwa hiyo nawashuhudia wote siku ya leo, kwamba sina hatia ya damu ya Myahudi wala Mgiriki, ambaye atapotea. Maana sikuepuka kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu, yaani kila mtu aweze kuokolewa na kupata uzima wa milele.

Jitunzeni nafsi zenu, na kondoo wote wa kanisa, Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa wachungaji wa kundi, ili mpate kulilisha kanisa Lake Mungu, Mali Yake Mwenyewe, alilyoinunua kwa damu Yake. Najua baada ya kuondoka kwangu watakuja mbwa wa mwitu miongoni mwenu wasilihurumie kundi, tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawafuate wao. Kesheni, mkikumbuka ya kwamba kwa miaka mitatu, usiku na mchana sikuacha kumwonya kila mtu kwa huzuni na machozi.

Paulo aliwapa watoto wake katika imani wosia "mafundisho ya uongo yasiyo kwenye Biblia yaja." Ila wajue Yesu Ndiye shabaha ya kuangalia, Paulo alikuwa na nia moja tu 'kumhubiri Yesu wake', Yule aliyekufa msalabani. Paulo akasema, nawaweka katika mikono ya Mungu, kwa Neno la Mungu na neema Yake yenye nguvu. Neno ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa. Sikuwa na tamaa na fedha au kitu chochote cha mtu. Ninyi wenyewe mnajua kwamba nimekuwa nikitengeneza mahema ili kukidhi mahitaji yangu, na ya wengine. Katika yote nilitaka kuwaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi, imewapasa kuwasaidia wanyonge na kuyakumbuka Maneno ya BWANA Yesu, aliyosema Mwenyewe "Ni heri kutoa kuliko kupokea."

Akisha kusema nao alipiga magoti na kuomba nao wote. Wote wakalia na kumwangukia shingoni wakimbusu na kuhuzunika zaidi kwa sababu ya Neno lile alilolisema ya kwamba hawatamwona tena uso Wake. Wakamsindikiza kupanda merikebu. Paulo alikuwa baba wa makanisa mengi, aliyosaidia kuanzisha. Akawapa mashauri na kuwaandikia. Hakujali maisha Yake, maana alijua kwamba maisha yana maana tu, tukijitoa kuwambia wengine kuhusu Habari njema na ufalme Wake. Ni jambo la kustaajabisha jinsi makanisa ya Kikristo yalivyoanza, na jinsi mitume walivyotia bidii usiku na mchana. Upendo wa Ndugu ni jambo la baraka sana. "Tazama jinsi ilivyo vema na kupendeza, Ndugu wakae pamoja, kwa umoja. Ni kama mafuta mazuri kichwani, Yashukayo ndevuni, ndevu za Haruni, Yashukayo mpaka upindo wa mavazi yake. Kama umande wa Hermoni ushukao milimani pa Sayuni. Maana ndiko BWANA alikoamuru baraka, Naam, uzima hata milele".

*Ombi la kila siku la Mzazi—Fanya kazi yako iwe ya kupendeza kwa nyimbo za sifa. Ikiwa ungependa kuwa na rekodi safi katika vitabu vya mbinguni, usikasirike wala kukemea. Acha sala yako ya kila siku iwe, "Bwana, nifundishe kutenda vyema. Nifundishe jinsi ya kufanya kazi bora. Nipe nguvu na uchangamfu." ... Mlete Kristo katika yote unayoyafanya. Ndipo maisha yenu yatajazwa na mwangaza na shukrani ....Hebu na tujitahidi, tukisonga mbele kwa uchangamfu katika utumishi wa Bwana, mioyo yetu ikiwa imesheheni furaha Yake.

----------------------------

Maswali: Jambo gani lilimpata Eutiko alipolala wakati wa mahubiri? Paulo alifanya nini kwa Eutiko baada ya hapo? Paulo alisema maneno gani ya kuwaaga waumini? Kwa nini waumini walilia machozi Paulo alipowaaga? Wachungaji wanakiukaje kazi ya kiuchungaji siku hizi za mwisho wa historia ya dunia?

**SIKU YA 316.**
**(Novemba 11)**

# Paulo akamatwa.

**Matendo 21**



Wakimaliza kuagana walipanda merikebu kwenda Kosi, mpaka Rodo, kisha Patara, pale wakapata meli inayoenda Foinike, wakaipanda na, wakaona kisiwa cha Kupro, na kusafiri mpaka Shamu, wakashuka Tiro. Meli ikashusha shehena pale, na wakakutana na waumini wengine, na kukaa siku saba, waumini kwa uwezo wa Roho Mtakatifu walitabiri wakimwambia Paulo asiende Yerusalemu. Baada ya hapo walienda na wale wahubiri, watoto, na wake zao na waumini wakaja mpaka nje ya mji, na kupiga magoti pwani wakaomba.

Wakapanda merikebuni na kufika Tolemai, wakawamkia ndugu katika Kristo kule na kuendelea Kaisaria. Hapa walikaa nyumbani mwa Filipo; huyu alikuwa kati ya wale mashemashi saba, mhubiri wa injili. Injili iliwakutanisha tena kwa urafiki na kuwa watenda kazi pamoja. Filipo alitoroka kwa ajili ya ile ghadhabu ya Sauli, ila Sauli alikuwa amekuwa Paulo sasa na walikuwa ndugu katika BWANA. Basi Filipo alikuwa na binti wanne mabikira waliokuwa manabii. Wakikaa pale kwa siku nyingi, akaja nabii mmoja aitwaye Agabo, ametoka Uyahudi, naye alipofika pale aliutwaa mshipi wa Paulo, na kujifunga miguu na mikono yake akisema “Roho Mtakatifu asema hivi, watamfunga mtu mwenye mshipi huu miguu na mikono, nao watamtia kwenye mikono ya watu wa mataifa, kumshitaki na kumwua.”

Basi wale wanafunzi au waumini akiwemo Daktari Luka na watenda kazi na Paulo waliposikia kwamba ataenda kuuwawa, walimsihi Paulo asipande kwenda Yerusalemu. Ndipo Paulo akajibu “mbona mnalia hivi, na kunivunja moyo? Kama Roho Mtakatifu anataka nifungwe, ni tayari hata kuuwawa Yerusalemu kwa ajili ya Jina la BWANA Yesu.” Waliposhindwa kumbadilisha mawazo yake, walinyamaza wakisema “mapenzi ya BWANA yatendeke.”

Wakatoka Kaisaria na kuchukua vitu vyao, na kutembea kwa mguu mpaka Yerusalemu. Baadhi ya wanafunzi au watenda kazi na Paulo wa Kaisaria walifuatana nao, kama Mnasoni, mtu wa Kipro mfuasi wa zamani ambaye walikaa

kwake Kaisaria. Walipofika Yerusalemu, ndugu katika Kristo waliwakaribisha kwa furaha na hata siku ya pili, Paulo akaingia kwa Yakobo ndugu wa Yesu pamoja na watumishi wengine kama tabibu Luka na wazee waliofanya kazi ya injili na Paulo. Ilikuwa imepita miaka kama 25 toka Yesu afufuke.

Watu wengi wa Yerusalemu walikuwa wameamua kumfuata Yesu. Wakawasalimia washiriki hawa na kuelezana mambo yote Mungu aliyotenda katika mataifa kwa huduma Yake, nao waliposikia wakamtukuza Mungu. Watu hawa wa mataifa walijisikia ni sehemu ya ufalme wa Mungu wakajibidisha hata kujitoa kwa hali na mali ili ndugu zao Wayahudi na watu wa dunia yote wapate injili. Walipopeana ripoti hizi, Wayahudi waliona kwamba wamerudisha nyuma kazi ya injili kwa mitazamo yao. Je, Leo unawasapoti watenda kazi aliowachagua Mungu hata wale ambao unafikiria wanafanya kazi kwa mtindo ambao wewe hukuuchagua?
Nao Wayahudi wakasema ya upande wao, wakiwaambia kwamba Mungu amewabariki katika Yerusalemu pia. Maelfu ya Wayahudi wamemwamini BWANA Yesu kama Masihi, na wana shauku ya kushika torati ya Musa zaidi, maana wamepata picha yote kamili. Wakamwambia jambo ambalo limekuwa na shida, ni kwamba walisikia habari zako, zilizosemwa kwamba Paulo aliwaambia watu wasiwatahiri watoto wao, wala wasizifuate desturi. Wakisema, waumini wakisikia umekuja, watakuja kuweka mkutano, kujadili haya yote, tuna hofu kwamba hili litaumiza kanisa.

Wakampa ushauri wao binafsi, maana hatuwezi kusema ulitoka mbinguni wakisema "achukue watu wanne, ambao wamekula kiapo cha kujitakasa na kujiweka wakfu, ujitakase nao, na kuwagharimia ile kodi ya hekalu. Wanyoe vichwa vyao, watu wote wapate kujua ya kuwa habari zile walizoambiwa juu yako hazina Ukweli." Ila wale Wayahudi bado walisisitiza watu wa mataifa waendelee kutunza sheria za Musa, japo watu wa mataifa walikubali wosia wa baraza "wajilinde na desturi za kipagani, za kutoa sadaka kwa sanamu, uasherati na kula nyama zilizosongolewa."
Paulo akakubali afuate ushauri wao, kwa kuwafurahisha tu ila ulikuwa uamuzi wa hatari. Kesho yake akatwaa wanaume wale na siku ya pili akajitakasa nafsi yake na akaenda nao pamoja na kuingia hekaluni, akitangaza habari ya kutimiza utakaso, hata sadaka itolewe kwa ajili ya kila mmoja wao. Pale hekaluni, kama kawaida yao walinyoa nywele na kumpa kuhani kuzichoma, na kutoa kafara zao. Ilipofika mwisho wa juma, na karibu wanamalizia zile siku zao za utakaso, wakatokea Wayahudi kutoa Asia ndogo wanatembelea hekalu la Yerusalemu.

Hawa walipomwona Paulo ndani ya hekalu, wakapiga kelele, kwa madai yasiyo ya kweli. Wakamkamata na kumsonda, jambo lililopelekea watu wamtazame na kuleta ghasia. Wayahudi hawa walisema "Enyi wanaume wa Israeli, tusaidieini, huyu ndiye mtu yule afundishaye watu wote kila mahali kinyume cha taifa letu na torati yetu, amewaingiza Wayunani katika hekalu akapatia unajisi mahali hapa patakatifu. Walisema hivi kwa vile walimwona Trofimo Mwefeso, pamoja nao mjini wiki hiyo, ambaye wakadhani Paulo amemwingiza katika hekalu na kumbe hakufanya vile.
Mji wote ukataharuki, watu wakakimbia mbio mbio, wakamkamata Paulo na kumkokota, wamtoe nje ya hekalu, na kufunga milango. Wakatafuta njia za kumwua hapo hapo, ila mtu alituma habari kwa Jemadari wa kikosi kwamba Yerusalemu

imechafuka. Jemedari akatwaa askari na maakida wakaenda mbio mbio, na watu walipoona kikosi kinaingia, waliacha kumpiga Paulo. Jemedari wa kikosi akamsogelea Paulo na kuamuru afungwe kwa minyororo miwili kama nabii Agabo alivyotabiri, akauliza “Ni nani huyu, na amefanya nini?” Yale makutano yakawa na vurugu, tupu, wengine wakisema hivi na wengine vile, hata wasijue wanasimamia nini.

Machafuko yakiendelea vile, yule Jemedari aliamuru Paulo apelekwe ndani ya ngome, ahojiwe kule. Maaskari hawa wa Kirumi ambao hawakumjua Mungu wa mbinguni, wakaitwa mapagani siku zile ndiyo walitaka kumlinda Paulo. Hawa walimchukua Paulo kumwepusha na hasira ya kutano lile, maana waliendeleza hasira na jazba za kupiga kelele, Paulo akichukuliwa. Walipofika kwenye ngazi, kuingia ngome ya Antonia, iliyotazama hekalu, maaskari ilibidi wambebe Paulo kwenye mabega yao kwa usalama wake, maana genge lile la watu lilikuwa na hasira wakitaka kumwua. Walijaribu kumfuata wakitaka kumpiga, na wakaendelea kupiga mayowe “Mwue, Mwue.”

Paulo Mfarisayo alishiriki kuuwawa kwa wengi waliompokea Yesu, sasa naye alikuwa hatarini kupoteza maisha yake kwa kuwa mwaminifu kwa Kristo ila Mungu alimpa ujasiri wa ajabu.

*Vijana waombe Kila Siku kwa ajili ya Hekima na Neema — Majaribu na ufukara ambao vijana wengi wanalalamikia, Kristo alivivumilia bila kunung’unika. Na nidhamu hii ndiyo ule uzoefu ambao vijana wanauhitaji, na ambao utawapa uthabiti katika tabia zao, na kuwafanya wawe kama Kristo, wenye nguvu katika roho ya kupinga majaribu. Hawataweza, ikiwa watajitenga na ushawishi wa wale ambao watawapotosha na kuharibu maadili yao, kushindwa na hila za Shetani. Kupitia maombi ya kila siku kwa MUNGU, watakuwa na hekima na neema kutoka Kwake ya kubeba migogoro na uhalisia mkali wa maisha, na kuwa washindi. Uadilifu na utulivu wa akili unaweza kutunzwa tu kwa kukesha na kuomba. Maisha ya Kristo yalikuwa kielelezo cha nguvu ya kudumu, ambacho hakikuruhusiwa kudhoofishwa na lawama, dhihaka, ufukara au shida. {

---------------------------

Maswali: Nabii Agabo alitabiri nini? Kwa nini watu walitaka Paulo auwawe? Je, yawezekana dini ya Kristo kuleta maumivu au kifo kwa wengine? Jemedari wa kikosi alimsaidiaje Paulo? Je, Kwa nini ni makosa kutaka kumwua mtu mwovu au asiye mwovu, tukifikiri kwamba tunamtumikia Mwenyezi Mungu? Kwa nini ushuhuda wetu ni ngazi nzuri ya kueneza kisa cha injili?

**SIKU YA 317.**
**(Novemba 12)**

# Paulo ajitetea na kurudia Historia ya injili.

**Matendo 21, na 22**

Paulo alipoletwa ndani ya ngome ya Antonia, alimwambia kwa Kiyunani Jemedari "Nina Neno, unaniruhusu nikuambie." Yule Jemedari akashangaa kwamba Paulo anajua Kiyunani, akamwambia "umejifunza wapi kuzungumza Kiyunani? Wewe si yule Mmisri ambaye kabla ya siku hizi aliwachukua watu elfu nne, walioitwa wauaji, akawaongoza jangwani kufanya uharamia?" Paulo akasema "Hapana mimi ni Myahudi, niliyezaliwa Tarso, mji wa Kilikia, mwenyeji wa mji usiokuwa mnyonge, unaoheshimiwa na Warumi, mimi si haramia au mwuaji. Nipe fursa niseme na wenyeji hawa." Jemedari alikubali kumpa ruhusa, akapunga mkono kwa makutano wawe kimya. Paulo akasimama darajani, yaani jukwaa lenye ngazi hivi, akapata nafasi ya kumshuhudia Yesu tena, kwa maelfu ya watu.

Paulo akaanza hotuba yake, akisema Enyi wanaume, ndugu zangu na baba zangu nisikilizeni, nikijitetea mbele yenu sasa. Watu walipomsikia akizungumza lugha ya Kiebrania wakazidi kunyamaza. Ndipo akaendelea akisema Mimi ni Myahudi, mwenzenu, nalizaliwa Tarso, mji wa Kilikia, ila nililelewa katika mji hapa hapa Yerusalemu, miguuni pa mwalimu Gamalieli, Rabi ambaye alinifundisha sheria, ya mababa zetu, na umuhimu wa torati ya Musa. Nilikuwa mtu wa jitihada niliyekereketwa na kumtumikia Mungu kama ninyi mlivyo leo. Nikawaudhi watu, kwa kuwatesa na kuwafunga gerezani waume kwa wake, nikifikiri ninamfanyia Mungu hisani, na ndicho Mungu anataka nifanye.

Kama mmoja wa baraza la Sanherdini na mnazarayo, niliendelea na kazi hii, hata kuhani mkuu na wajumbe wa baraza wananijua. Maana ndiyo wao walinipa mamlaka ya kufanya uovu huo. Walinipa barua ya kibali toka kwao kwenda Dameski, ili niwalete wale waumini wanaomwamini Yesu aliyefufuka, waje hapa Yerusalemu, hali wamefungwa ili waadhibiwe. Ikawa nilipokuwa nakaribia Dameski, katika safari yangu, mchana wa sasa sita, ghafla nikaona nuru kuu kutoka mbinguni, ikinimulikia pande zote, nami nikaanguka. Kisha nikasikia sauti "Sauli Sauli mbona unanitesa?" Nami nikajibu "U nani Wewe BWANA?" Akaniambia Mimi ni Yesu Mnazareti, Ambaye wewe unaniudhi? Wale tuliokuwa tumesafiri pamoja nao waliiona ile nuru, na kusikia sauti, ila hawakuweza kuelewa Maneno yale. Nikauliza nifanye nini BWANA? ndipo BWANA akaniambia nisimane na kuingia mji wa Dameski, na huko nitaambiwa yote yaliyoamriwa niyafanye.

Nikawa kipofu, kwa sababu ya nuru ile. Nilishikwa mikono na watu nikiongozwa na wenzangu waliokuwa pamoja nami, tukafika Dameski. Hapa ndipo mtauwa wa Mungu, aliyeshika na kufuata Sheria na kushuhudiwa wema na Wayahudi wote waliokaa huko Damesiki alikuja. Huyu alisimama karibu nami akisema "Ndugu yangu Sauli, uone", nikainua macho yangu na kuona saa ile ile. Akaniambia

“Mungu amekuchagua wewe upate kujua Mapenzi Yake na kumwona mwenye haki na kuisikia sauti itokayo katika kinywa chake. Maana utakuwa shahidi wangu kwa watu wote Wayahudi na wa mataifa, kwa mambo yote uliyoyaona na kuyasikia. Basi sasa unakawia kwa nini? Simama ubatizwe, ukaoshe dhambi zako na kuliitia Jina la BWANA ili akuokoe.”

Ikawa niliporudi Yerusalemu baada ya miaka mitatu, nikisali katika hekalu nikiwa na hali ya kuzimia roho nikapata maono na kumwona Yesu. Naye Yesu akaniambia “Hima utoke Yerusalemu upesi, usianze kunishuhudia hapa kwani watu hawatakubali ushuhuda wako katika habari zangu.” Nami nikasema BWANA wanajua hao ya kuwa mimi nalikuwa mkatili kwa waumini hapa nikiwafunga wote gerezani wanaotaka kuamini na kuwapiga katika kila sinagogi. Na wakati Stefano anauwawa, shahidi wako wa Kweli, damu yake ikimwagika mimi nami nilikuwa karibu, nikionyesha kwamba nakubaliana na uovu wao kwa kunyamaza kimya, nikilinda makoti ya wale ambao walikuwa wanatupa mawe kumwua. BWANA akaniambia enenda zako kwa kuwa Mimi nimekutuma uende mbali kwa mataifa, nimekufanya uwe chombo kiteule na ushuhuda kwa wale ambao hawakunijua.

Walimsikliza mpaka alipoanza kusema “mataifa”, ghadhabu ikawashika na wakapaza sauti zao wakisema “mwueni, huyu kwa maana hafai kuishi” wakawa kama wanyama wakali waliokosa kutawala nafsi. Wakiendelea kupiga mayowe, wakatupa mavazi yao, na kurusha mavumbi juu. Yule Jemedari aliamua Paulo aletwe ndani ya ngome”

*Ndivyo inavyopaswa kuwa kwa vijana. Ikiwa Majaribu yataongezeka juu yao, wanaweza kujua kwamba MUNGU anajaribu na kudhihirisha uaminifu wao. Na ni katika kiwango hicho tu ambacho wanadumisha uadilifu wao wa tabia katika mazingira ya kukatishwa tamaa, ndipo uimara, ujasiri, uthabiti, na uwezo wao wa kustahimili utakapoongezeka, nao watakuwa na nguvu katika roho.
------------------------------

Maswali: Paulo alikuwa mzaliwa wa wapi? Kwa nini Paulo alirudia historia ya ushuhuda wake? Kwa nini Jemedari alishangaa Paulo alipozungumza naye? Paulo alisemaje kuhusu kifo cha Stefano?

**SIKU YA 318.**
**(Novemba 13)**

# Masadukayo na Mafarisayo wamgombania Paulo.

**Matendo 22-23**



Jemadari yule akaamuru Paulo aletwe ndani na kuulizwa habari zake kwa kupigwa bakora, mpaka akiri kwa sababu gani watu wale wakampigia kelele na kumchukia kiasi kile. Wakati walinzi wanamfunga kamba na kumtoa nje ili kujitayarisha kumpiga bakora, akamwona akida na kumwuliza swali "Je ni halali ninyi kumpiga raia wa Rumi kabla hajahukumiwa?" Yule akida aliposikia alishangaa na kwenda kumwarifu yule Jemedari aliyetoa ile amri akisema "Bwana, lazima tuwe waangalifu na tunachomtendea huyu bwana maana anadai ni raia wa Rumi."

Siku zile kwa vile Rumi ilitawala karibu dunia yote, raia wake walikuwa na sheria na maslahi tofauti yanayowalinda zaidi kuliko raia wa nchi zile zinazotawaliwa. Ni kama tulivyotawaliwa na Mfaransa au Mwingereza, raia wake akikosa, anayekaa nchi hizo, asingehukumiwa kama Mwafrika mwingine. Jemedari akaenda kumwuliza Paulo "Je wewe ni raia wa Rumi?" Paulo aliitikia "Ndiyo."Yule Jemedari alisema, hata

yeye ni raia wa Rumi, ila alitoa mali nyingi kununua uraia huu. Paulo akamwambia yeye ni Mrumi kwa kuzaliwa wala hakuwa na haja ya kulipia pesa.

Wale waliokuwa tayari kumtesa na kumpiga, wakapotea, wakamwacha. Na yule Jemedari akaogopa maana amemweka raia wa Rumi vifungoni bila ya kumpa haki ya kujitetea kimahakama. Akawaambia askari Jela watoe pingu zake. Siku ya pili yake akitaka kujua kwa hakika ni kwa nini Wayahudi wamemshitaki, akamfungua na kuwaita wakuu wa makuhani na baraza la Sanhedrini wakutane, na akamwita Paulo mbele yao ajitetee. Paulo akawakazia macho wazee wa baraza na kusema, ndugu zangu, nimeishi mbele za Mungu na watu na dhamiri safi kabisa hata hivi leo.

Kuhani mkuu Anania akamuru wale walio karibu na Paulo wampige mdomo kumnyamazisha. Yaonekana hii ndiyo ilikuwa tabia ya viongozi wa dini kuwafanyia ukatili watu wa kawaida, wasio na cheo au mali, kwani ndicho walichomfanyia Yesu pia. Ndipo Paulo akasema "Mungu atakuadhibu kwa hili, unadirikije kumwambia mtu huyu anipige, umeketi kutetea sheria na haijahakikishwa kama nimetenda ovu, nawe unaamuru nipigwe kinyume cha sheria? Mungu atakupiga wewe, ukuta uliopakwa chokaa."

Wale waliosimama karibu yake wakasema kumfurahisha Yule kiongozi wa dini mwovu anayepokea mshahara wa pesa za nyumba ya Mungu bali anamtumikia Ibilisi "Je unamtukana kuhani mkuu wa Mungu?" Maskini watu wale hawakujua Paulo ndiye kuhani wa Mungu, bali yule kuhani mkuu alikuwa wa jina tu, au mtumishi wa mshahara, yaani alimtumikia Ibilisi. Tukumbuke hata viongozi waovu, wanapaswa kuheshimiwa, ila katika kuwaheshimu huko, tusivunje Sheria za Mungu. Hebu tuwajibu kwa adabu.

Basi Paulo akajibu "samahani sikujua, ndugu zangu ya kuwa yeye ni kuhani Mkuu maana imeandikwa, kwenye Sheria ya Musa usimnenee mabaya mkuu wa watu wako" hata akiwa mwovu. Paulo akatambua katika baraza lile, kuna watu wa aina mbili, mafarisayo na masadukayo, akaona ni vizuri awatenganishe ili apate usikivu wao. Akasema "Ndugu zangu mimi ni Farisayo, na mwana wa Farisayo; mimi nahukumiwa kwa ajili ya tumaini la ufufuo wa wafu."

Masadukayo hawaamini ufufuo, kiyama, roho, mbingu au maisha yajayo au malaika au vitu vilivyo mbinguni. Mafarisayo wao wanaamini yote ya kwenye Biblia au Maandiko Matakatifu ila ni wanafiki, hawatendi Maandiko, bali wataka wengine watende. Hawa huona wanashika sheria kuliko wengine, bali wana kiburi, na hupenda kuumiza wengine kwa kifupi, hawana upendo. Makuhani wengi siku zile walikuwa masadukayo. Jambo la kushangaza, maana kama hawaamini vitu vya mbinguni wala ufufuo, basi sidhani kama wangeamini chochote cha maana tunachojua waumini leo toka kwenye Neno la Mungu.

Basi yale makundi kusikia vile, palikuwa na mashindano kati yao, yaani mafarisayo na masadukayo, wakafarakana. Mafarisayo wengine wakasema "hatuoni uovu wowote katika mtu huyu; pengine Roho wa Mungu au malaika amesema naye,

hebu tusimpinge Mungu." Ugomvi mkubwa ukatokea na wengine mafarisayo wakamvuta Paulo aende upande huu, na huku masadukayo wakitaka aende upande ule. Wakawa na fujo na kutumia nguvu mpaka Jemedari akachelea Paulo asije akararuliwa vipande viwili nao. Akaamuru kikosi cha askari kije kuleta amani, na washuke na kumwondoa Paulo mikononi mwao na kumleta ndani ya ngome.

*Haja ya Mwalimu Kusali Kila Siku—Kila mwalimu anapaswa kupokea kila siku mafundisho kutoka kwa Kristo na anapaswa kufanya kazi daima chini ya uongozi Wake. Haiwezekani kwake kuelewa vizuri au kufanya kazi yake ipasavyo isipokuwa anakuwa na Mungu katika maombi mengi. Ni kwa msaada wa Bwana tu, pamoja na unyofu wa moyo , na juhudi katika kujikana, ndipo anaweza kutumaini kufanya kazi yake kwa busara na vizuri zaidi.
------------------------------

Maswali: Kwa nini Jemedari aliacha kumpiga bakora Paulo? Je, siku hizi kuna mafarisayo na masadukayo wanaogombania imani zao? Je, ni halali mchungaji kumpiga kofi mtu kama Paulo alivyopigwa na kuhani? Kwa nini Paulo aliomba samahani japo alikosewa?

**SIKU YA 319.**
**(Novemba 14)**

# Paulo aenda Kaisaria na Jeshi.

**Matendo 23**

Usiku ule BWANA Mwenyewe akasimama karibu na Paulo, akimfariji kwa kumwambia "uwe na moyo mkuu; kwa sababu kama ulivyonishuhudia habari Zangu Yerusalemu, imekupasa kunishuhudia ushuhuda huo huo Rumi." Kulipopambazuka, zaidi ya wanaume wa Kiyahudi 40 walifanya mapatano wakaapa kiapo kwamba hawatakula wala hawatakunywa mpaka wamwue Paulo. Baada ya makubaliano hayo, walienda kwa wakuu wa makuhani na wazee wakawaambia kwamba wamekula kiapo, hawataonja kitu, hata kunywa maji, mpaka wamwue Paulo. Wakaomba wale wazee na makuhani wafanye mpango na Jemadari wa Kirumi kumleta Paulo kwenye baraza tena, mara moja tu. Walijidai wanataka kujua habari zake zaidi. Kumbe ilikuwa ni njama ya kumwua haraka wakati analetwa, hata kabla hajapanda kwenye jukwaa.

Mpwa wake Paulo, mtoto wa dadaye alisikia habari hiyo na alipomwambia mamaye, mamaye alimtuma aende ngomeni kumwambia Paulo uovu ule. Paulo akamwita akida au askari Jela na kumwambia mmoja wao, amchukue yule kijana aende naye kwa Jemedari maana ana neno la kumwarifu Jemedari. Basi yule askari Jela akamchukua yule kijana na kumpeleka kwa Jemedari akisema "Paulo yule mfungwa aliniita na akataka nikuletee huyu kijana ana neno la dharura la kukwambia." Yule Jemedari alimshika mkono yule kijana akampeleka kando na kumwuliza ana taarifa gani? Yule kijana akamweleza, kwamba habari zimeenea kwa jumuiya ya Wayahudi na watu wamekula kiapo jinsi watakavyokwenda kwake Jemedari kesho ili kumwua Paulo. Akamwelezea Jemedari njama yote. Jemadari alipoachana na kijana, alimweleza asimwambie mtu awaye yoyote kwamba "umeniarifu haya, asante nenda sasa." Hakika kuwa mwanafunzi wa Yesu uhusisha gharama ya imani na utii.

Jemedari aliita askari wawili na kuwaambia waweke tayari askari saa tatu ya usiku. Askari mia mbili wa miguu, askari sabini wapanda farasi, na askari mia mbili wa mikuki kwenda Kaisaria. Akawaambia waweke farasi pia wa kumpandisha Paulo na mwingine wa kuchukua mizigo aliyo nayo salama kwa Feliki Gavana wa Kirumi. Kisha akamwandikia Feliki barua. Paulo aliona mengi akimtumikia Mungu. Kikosi cha watu 470 kikamsindikiza mtu wa Mungu mpaka Kaisaria kwa Gavana kwani Mungu alitaka asipate madhara mpaka atakapomaliza kazi aliyompa. Hata nasi leo Mungu atatufanyia makubwa, akitulinda, tukiamua kujitoa kufanya kazi Yake. Barua kwa Feliki kutoka kwa "Klaudio Lisa Jemedari, kwa Gavana Feliki mtukufu, salamu, siku chache mtu huyu alikamatwa na Wayahudi, wakawa karibu kumwua, ndipo nikaandaa pamoja na kikosi cha askari kumwokoa, na hapo ndipo nilipata habari kwamba yeye ni Mrumi. Nami nikataka kujua lile Neno walilomshtakia, nikamtelemsha, na kumweka mbele ya baraza la Wayahudi la Sanhedrin.

Nikagundua kwamba ameshitakiwa bila uhalifu wowote. Nikagundua mashitaka yalikuwa maswali ya sheria yao Wayahudi, na wala hakustaili kuuwawa wala kufungwa. Ndipo mchana huu nilipopokea habari kwamba patakuwa na njama juu ya mtu huyu kumwua kesho. Nikaamua nimlete kwako, nikaagiza wale waliomshtaki, wanene habari zake mbele yako huko Kaisaria. Wasalamu."

Basi wale maaskari wakamchukua Paulo kama ilivyoamriwa saa tatu usiku, na kumpeleka Antipatri kilomita 45 kutoka Yerusalemu, hata asubuhi wakawaacha wale wapanda farasi 70 waendelee pamoja naye, na wale wanaotembea kwa miguu 400 wakapumzika na kurudi Yerusalemu. Kile kikosi cha Jeshi cha wapanda farasi kikaendelea na Paulo na walipofika Kaisaria wakaenda kumpa barua yule Gavana wakamtoa Paulo kwa gavana huyu kama Jemedari alivyoandika. Gavana alisoma barua na kumwuliza Paulo, ni mwenyeji wa wapi? Naye akarudia kusema kwamba anatoka Tarso, Asia ndogo. Gavana akamwambia, atamweka hapa chini ya ulinzi katika jumba la gavana, ambalo Herodi alilijenga. Unajua kile kilichotokea kwa wale watu waliokula kiapo wasile mpaka wamuue Paulo? Pengine walifungua saumu yao wakala, sidhani kama walijiua kwa namna ile ya kutokula au kunywa maji. Tuwe waangalifu sana kuhusu viapo ambavyo ni vya kijinga au haviendani na Neno la Mungu.

*Maombi ya Kila Siku Hustawisha na kuboresha Uzoefu Wetu wa kiroho—Dini lazima ianze kwa kusafisha na kutakasa moyo, na lazima ipewe lishe kwa maombi ya kila siku.


--------------------------

Maswali: Malaika alimwambiaje Paulo kwenye maono? Mpwa wa Paulo alikuwa na ujumbe gani? Paulo alisindikizwa na watu wangapi? Gavana alimwuliza maswali gani Paulo?

**SIKU YA 320.**
**(Novemba 15)**

# Paulo mbele ya Gavana Feliki.

**Matendo 24.**



Baada ya siku tano, Kuhani mkuu na baadhi ya wazee wa baraza la Sanhedrin, na Tertulo mwanasheria wa baraza walifikia Kaisari kumwona Gavana kuhusu mashitaka ya Paulo. Hawa wakamweleza Gavana habari za Paulo. Gavana alipowapa nafasi, Tertulo msemaji maarufu akaleta mashitaka akianza kumsalimu Gavana kwa kumpaka mafuta kwa mgongo wa chupa "Ee Feliki mtukufu, ni chini ya utawala wako wa hekima ndiyo maana tunapata amani nyingi, chini yako kwenye taifa hili, mambo mabaya yanakarabatiwa, na mapinduzi mengi yanatendeka kusaidia watu wema. Tunaukaribisha utawala wako, kila mahali na wakati wowote. Tunashukuru kwa kuwepo kwako hapa, Ee mtukufu Feliki.

Hatutaki kukuchosha kwa kuchukua muda wako mwingi, ila tunasihi utusikilize kwa maneno machache na kwa fadhili zako kwa kifupi kuhusu mashitaka ya mtu huyu Paulo. Tumemwona kuwa ni mtu mkorofi na wa hatari, anayeanzisha fitina katika Wayahudi wote duniani, tena ni kiongozi wa genge la watu wa dini waitwayo Wanazarayo. Alikuwa analitia hekalu unajisi kwa makusudi, tukamkamata, na tunataka tumkuhumu kwa sheria yetu. Lakini Lisia Jemedari akamwondoa mikononi mwetu kwa nguvu, na akaleta kikosi kilichomnyakua toka mikono yetu.

Lisia aliamuru kama tunataka kumshataki, tuje hapa Kaisaria. Kama unaweza mwenyewe kumwuliza mshatakiwa, unaweza kupata habari ya mambo yale yote tunayomshtaki sisi." Kwa kweli Feliki hakuleta amani yoyote na hakuwa muungwana au mtukufu kama mwanasheria alivyomsifu. Alipomalizia Tertulo, mwanasheria anayetetea Sanhedrin, alisema awaulize hata ule msafara waliokuja nao watasema ndiyo. Basi Wayahudi waliokuwa pale nao walisema ndiyo.

Gavana akampungia mkono Paulo azungumze akijitetea akiamini alikuwa hana hatia. Paulo alianza kwa kusema kwamba ninajua wewe Mkuu umekuwa mwamuzi wa taifa hili kwa miaka mingi, na umesikia kesi mbali mbali zinazohusu Wayahudi, hivyo nitajitetea mwenyewe kwa moyo wa furaha. Paulo akaendelea kusema yapata siku 12 hivi alienda Yerusalemu kuabudu, watu hawa Wayahudi hawakuniona ndani ya hekalu nikihojiana na mtu au kufanya fujo au fitina katika mkutano wala katika masinagogi au ndani ya mji. Wala hawataweza kuyahakisha wasemayo wanayonishitaki sasa. Ila nina neno la kukiri mbele yako kwamba namwabudu Mungu wa baba zangu, jinsi ambayo Wayahudi huita uzushi.

Naamini kile Musa alisema na mitume wote waliyoyaandika, ikiwemo na unabii wa Masihi. Nina matumaini kwa Mungu kama tu yale waliyonayo na wanayotazamia ya ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki siku ya mwisho, na kwamba sote tutasimama mbele ya hukumu kwenye kiti cha enzi cha Mungu kutoa hesabu ya mambo yote tuliyoyafanya. Ndiyo maana najizoeza katika Neno hili kwa kutenda bila hila ili niwe na dhamira isiyo na hatia mbele za Mungu na mbele ya watu siku zote.

Baada ya kuwa nje ya nchi yangu kwa miaka mingi, niliazimu nije ili niabudu, na niwaletee watu wa taifa langu sadaka na matoleo, niliyopewa na watu toka makanisa ya sehemu mbali mbali za himaya ya Rumi, ambao walijali hali za ndugu zao masikini wa Yerusalemu. Waliponiona ndani ya hekalu nikishugulikia jambo hili, hali nimetakaswa, wala sikuwa na mkutano wala ghasia, ila walikuweko Wayahudi wa kutoka Asia ndogo hawa, ambao wapaswa kuwepo hapa leo, ili watoe ushahidi. Hawa waliponiona walinishika na kunivuruta, na hii ikaanzisha vurugu. Hebu watu hawa na waseme sasa kama ni kosa gani waliliona kwangu, niliposimama mbele ya baraza. Kile ambacho wanaweza kunishitaki leo, ni kwamba naamini ufufuo wa wafu.

Akisema hivi masadukayo na mafarisayo wakaanza tena kubishana, na hawakupatana kwamba wanamshitaki kwa jambo gani. Paulo alipomaliza kuzungumza, Feliki akiwajua vizuri wafuasi wa Kristro, alifunga mjadala na kusema "Lisia Jemadari atakapotelemka, nitawasikiliza kwa undani na kuamua maneno yenu." Feliki alikuwa karibu na ufalme wa Mungu, bali alikuwa mbali nao, yaani alikosa ufalme wa Mungu kwa hatua chache sana. Akaamuru Paulo achukuliwe na askari na alindwe, ila awe na uhuru wa marafiki kumtembelea na kumhudumia.

*Ikiwa huhisi kwamba uko katika hatari yoyote, na ikiwa hautoi sala yoyote ya usaidizi wa nguvu za kupinga majaribu, utakuwa na uhakika wa kupotoka; Kupuuzia kwako wajibu kutarekodiwa katika kitabu cha MUNGU mbinguni, nawe utaonekana

kuwa umepungua katika siku ile ya hukumu.

*Akina baba na akina mama, hata kama unafanya biashara yako, usishindwe kukusanya familia yako karibu na madhabahu ya MUNGU. Omba ulinzi wa malaika watakatifu nyumbani mwako. Kumbuka kwamba wapendwa wako wanakabiliwa na vishawishi.

-------------------------

Maswali: Kuhani mkuu, baraza la wazee na mwanasheria walienda Kaisaria kufanya nini? Kwa nini Feliki alisema "njoo kesho" akijua hata kesho hatatoa ufumbuzi? Kwa nini ni dhambi kumwambia mtu, 'njoo kesho, njoo kesho' na una uwezo wa kumsaidia leo nawe humsaidii? Kwa nini Paulo alishitakiwa? Watu wa siku zile baada ya Yesu kufa walipata shida ya kueleza injili ya Yesu ambayo ilikuwa mpya japo ni ya toka kuwekwa misingi ya dunia? Leo ni miaka 2000 toka haya yalitokea, Je, tuna shida gani za kueneza injili leo pia?

**SIKU YA 321**
**(Novemba 16)**

# Paulo anakata rufani kwenda Rumi mbele ya Agripa.

**Matendo 24 na 25.**



Baada ya siku kadhaa Feliki alifika na mkewe Drusila ambaye alikuwa Myahudi, na akatuma Paulo aletwe, amsikilize akiwa peke yake na kumwuliza kuhusu imani yake kwa Yesu Kristo. Paulo alivyoshuhudia kwake kuhusu haki, kuwa na kiasi na kutawala nafsi na hukumu ya Mungu inayokuja na inayomngoja kila binadamu, hata naye, Feliki alipata hofu. Akitetemeka, asiweze kuvumilia alisema "waweza kwenda zako sasa Paulo, nikipata nafasi nitakuita tena." Alisema hivi kwa vile dhamiri yake ilimshtaki kwa hubiri lile, ila aliogopa kujisalimisha maisha yake kwa Mungu.

Alitaka kuwa mtu mkubwa bado, na Mungu awe ngazi ya chini yake. Isitoshe alitarajia rushwa toka kwa Paulo, ndipo amtoe kifungoni. Kupokea rushwa ni dhambi, kwani hupoteza haki ya mtu. Paulo alikuwa masikini wa kipato akitengeneza mahema. Gavana alikuwa mtu tajiri na bado alitaka kumdhulumu masikini. Basi akamwita Paulo mara nyingi akaongea naye, na miaka miwili ilipita. Masikini mtu wa Mungu akanyimwa haki yake ya kuwa huru. Feliki akitaka Wayahudi wampende alimwacha Paulo kizimbani. Mwishowe Felix alifukuzwa kazi na Gavana mwingine alichaguliwa badala ya yake, aitwaye Prokio Festo.

Baada ya siku tatu za kuwa Gavana wa Kaisaria, Festo alienda kutembelea Yerusalemu na kule kuhani mkuu na wazee wa baraza walimwambia kuhusu mashitaka ya Paulo na kumsihi ayatatue, kwa kumleta Paulo Yerusalemu wapate kupanga kumwua njiani. Walifanya hivyo kwa kuwa waliona serikali haitafanya lolote maana hayakuwa makosa ya jinai bali ni ya dini yao Wayahudi. Festo aliwaambia, Paulo analindwa na Kaisaria wa Rumi kama Mrumi, na yeye mwenyewe yu tayari kwenda huko kushughulikia hiyo kesi, Kwa nini wasije wakiwa tayari Kaisaria na

kuleta mashitaka.

Akawaambia wahusika wenye mamlaka warudi naye atakaporudi ili wafanye hiyo shughuli ya kumshtaki siku inayofuata Paulo kama ana neno lolote baya. Festo alikaa siku kumi na kwenda Kaisaria, na siku ya pili yake, akatunza neno lake, akaketi katika kiti cha hukumu na kuamuru Paulo aletwe. Wale Wayahudi waliokuja toka Yerusalemu na Festo wakaleta mashitaka mengi mazito juu yake, hata wakasema yu dhidhi ya Kaisari. Walisema mengi wasiyoweza kuyahakikishwa. Paulo alijijitetea vyema akisema "mimi sikukosa neno juu ya sheria ya Wayahudi wala Kaisari, kama ujuavyo mkuu Festo, siogopi kufa kama nastahili, ila si kweli maneno haya wanayonishitaki, hapana awezaye kunitia mikononi mwao.

Festo akitaka awafurahishe Wayahudi ili atunze urafiki nao, akamwambia Paulo kama anataka kwenda Yerusalemu nao, ili ajitetee kule. Paulo alisema alishapitia huko tayari, na hawakuweza kuhakikisha yale mashitaka hata moja isitoshe hakuna uhakika wa kupata hukumu ya haki, au kufika kwa usalama Yerusalemu hivyo naomba "kukata rufaa nimwone Kaisari Rumi." Festo akazungumza na watu wa Baraza la Sanhedrini wa Yerusalemu, na akamwambia Paulo "umekata rufani kama Mrumi, kwenda kwa Kaisari! Basi utakwenda kwa Kaisari." Akamaliza hukumu na kuwaambia watu watawanyike. Ilikuwa salama Paulo kuwa na watu wapagani wa mataifa Warumi kuliko waumini waliomjua Mungu vizuri ila walikuwa hawajajisalimisha Kwake.

Agripa alikuwa mwana wa Herodi aliyemwua Yakobo mtume mfia dini wa kwanza na kumweka Petro gerezani. Kaka ya babu wa babaye (Herode) ndiye aliyemwua Yohana Mbatizaji na kumkejeli Yesu wakati walipomhukumu kufa. Babu wa babaye (Herode) ndiye aliyeua watoto wa Bethlehemu baada ya Yesu kuzaliwa. Ilikuwa familia yenye ukatili mno ikiongozwa na adui wa Mungu. Mkewe Agripa aliitwa Bernike, basi wakaja naye Kaisaria kumtembelea Festo, ili kumsalimia na kumpa hongera kwa kuchaguliwa kuwa gavana.

Wakakaa pale kwa siku nyingi, na Festo akamweleza Agripa kuhusu Paulo, aliyeachwa kifungoni na Feliki. Akaeleza alipokuwa Yerusalemu wakuu wa makuhani na wazee wa Wayahudi walimwarifu habari zake, wakitaka amhukumu kwa mashitaka ya uhalifu kwao Wayahudi na Kaisari, ila niliwaambia kwamba si destruri yetu Warumi kuwapa mshitakiwa kuwafurahisha tu, kabla ya kumpa nafasi ya kukutana nao uso kwa uso na wanaomshtaki ili ajitetee kisheria. Hivyo tulipanga nao nikitoka Yerusalemu waje nami na keshoye tufanye mahakama, na kumwita mfungwa huyu awaone washitaki wake na kujitetea mashitaka yale wanayomtuhumu.

Wale Wayahudi waliposema hoja zao, hawakumshitaki kwa lolote baya la uhalifu nilivyodhani, bali walikuwa a maswali mengine mengine juu ya dini yao wenyewe na habari za mtu aitwaye Yesu Kristo, Ambaye miaka michache iliyopita alitundikwa msalabani chini ya Pilato, Paulo akasema Mtu huyu alifufuka katika wafu na anaishi sasa mbinguni. Kwa vile sikuwa na jinsi ya kuhukumu au kupeleleza hili, nilipata mashaka nifanyeje nikaona basi aende Yerusalemu ahukumiwe huko na Wayahudi. Ila mfungwa mwenyewe sasa amekata rufaa kwamba anataka kesi yake iende kwa

Kaisari, kwenye korti ya Rumi; basi nikaagiza alindwe hata watakapompelea kwa Kaisari. Mfalme Agripa akapata naye shauku, akasema angependa kumsikia mtu huyu. Festo akasema kesho atapata nafasi ya kumsikia.

Keshoye Agripa akaja na Bernike na furaha nyingi na tamasha za kujionyesha, wakaingia kusikia maneno pamoja na maakida wakuu na watu wakuu wa mji. Festo akatoa amri askari amlete Paulo. Festo akazungumza kwa wale wageni na watu wa mamlaka akisema "mfalme Agripa, na ninyi nyote mlio hapa nasi, huyu mtu ndiye Wayahudi walimshitaki kwa uhalifu kwenye hekalu lao. Wamenisihi hapa na Yerusalemu nimhukumu kifo. Nilipompeleleza, nikaona hakuna alichofanya kutokana na sheria yetu, cha kumfanya afe. Ila yeye ni raia wa Rumi, na amekata rufaa kwenda Rumi, kusikilizwa kesi yake kule. Hana makosa ya kuhukumiwa hapa, ila nimemleta mbele yenu wote, na hasa kwa mfalme Agripa, kuona jinsi mtakavyonisaidia kuandika barua kwa Kaisaria kadiri utakavyomhoji, kabla sijamtuma kule Rumi.

Kwa maana naona ni neno lisilo na maana kumpeleka mfungwa Rumi, bila kuonyesha mashitaka yake, hata wale watu wataona kwamba hatutumii busara. Agripa alimwambia Paulo ana ruhusa kusema maneno yake ya kujitetea. Hapa Paulo akapata nafasi nyingine ya kushuhudia. Mungu alitoa mlango wa Paulo kushuhudia kwa maelfu kwa njia hii na aliifanya vizuri. Alipata jukwaa la maelfu kumsikiliza ili wasitoe visababu siku ya hukumu. Kwani habari njema itahubiriwa kuwa ushuhuda, ili mtu asiseme hakusikia. Si lazima mtu aamue kumfuata Mungu na Mwana Wake Masihi, maana ni uchaguzi wa hiyari wa mtu. Mwenyezi Mungu hutoa nafasi kwa kila mtu kusikia habari njema za upendo Wake, na hivyo hakuna atakayetoa udhuru kwamba hakusikia siku ya hukumu.

*Katika jitihada zetu za kuwafariji na kuwafurahisha wageni, hebu tusipuuze wajibu wetu kwa MUNGU. Saa ya maombi haipaswi kupuuzwa kwa kuzingatia jambo au mtu yeyote. Msizungumze na kujifurahisha wenyewe hadi mjichoshe na kuwa hoi kabisa kufurahia msimu wa ibada. Kufanya hivi ni kumtolea MUNGU sadaka iliyo kilema. Katika Saa ya mapema ya jioni, tunapoweza kusali bila haraka na kwa uwazi wa kuelewa mambo ubongoni mwetu vyema, tunapaswa kutoa dua zetu na kupaza sauti zetu kwa furaha na sifa ya shukrani.
----------------------------------

Maswali: Kwa nini Feliki alitaka kupokea rushwa? Kwa nini Feliki alitetemeka? Herode Agripa alikuja Kaisari kufanya nini? Kwa nini Feliki alitaka kuwafurahisha Wayahudi? Je, leo wewe wataka kumfurahisha nani? Kwa nini Paulo alitaka kukata rufaa? Kwa nini Paulo alitolewa kwa Agripa ili azungumze? Bernike alikuwa nani? Kwa nini Wayahudi hawakumshitaki Paulo kwa uhalifu? Je Kwa nini mara nyingine ni salama kuwa na watu wasiomjua Mungu kuliko wale wanaomjua Mungu?

**SIKU YA 322.**
**(Novemba 17)**

# Paulo ashuhudia kisa chake tena.

**Matendo 26**

Paulo akapunga mkono wake, kama ishara akajitetea alipopewa ruhusa. Akasema, najiona nafsi yangu kuwa na heri kwa kupata nafasi ya kujitetea mbele yako leo, katika yale mambo niliyoshitakiwa na Wayahudi, hasa kwa sababu wewe unajua destruri, dini na maswali yote yanayohusu Wayahudi. Nakuomba unisikilize kwa uvumilivu, kwa maana Wayahudi wote, wanajua maisha yangu tangu ujana, yaliyokuwa tangu mwanzo katika taifa langu Yerusalemu. Wao wananijua sana toka mwanzo kama wakipenda kunishuhudia kweli, ya kwamba nalikuwa farisayo kwa kuifuata madhehebu ya dini yetu ya Kiyahudi iliyo sahihi kabisa, na sasa ninasimama hapa ili nihukumiwe kwa sababu ya tumaini la ahadi baba zetu waliyopewa na Mungu.

Tumaini ambalo kabila zetu kumi na mbili wanataraji kuifikia, wakimwabudu Mungu kwa bidii mchana na usiku, nami ninashitakiwa na Wayahudi kwa ajili ya tumaini hilo, la Masihi na kufa na kufufuka Kwake. Kwa nini limedhaniwa kwenu kuwa ni Neno lisilosadikika kwamba Mungu awafufua wafu? Kweli mimi mwenyewe naliona ndani ya nafsi yangu yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopingana na Jina Lake Yesu Mnazareti, kwa kuwaangamiza wote wanaomwamini Yesu, Ambaye Pilato alimsulubisha. Nilifanya haya Yerusalemu, kwa kuwafunga wengi watakatifu na nikapewa kibali na kuhani mkuu na nikaenda kwenye masinagogi nikiwaadhibu, kwa kuwashurutisha kukufuru. Niliwang'akia hasira yangu kama mwenye wazimu, nikawaudhi hata katika miji ya ugeni nje ya Israeli. Wale waliouwawa nilikubaliana na jambo hilo. Hili halikutokea mara moja ila mara nyingi.

Basi katika kazi hii ya uovu, nilipokuwa njiani kwenda Dameski na kibali cha kutesa Wakristo, kutoka kwa kuhani ndio mwangaza mkali ulinimulika kutoka mbinguni na nikapata upofu, na wote waliokuwa nami pia walianguka chini kwani waliouona mwanga na kusikia ngurumo. Nilisikia sauti kwa Kiebrania ikisema "Sauli Sauli mbona waniudhi, unakuwa kama ng'ombe mwenye wazimu anayepiga mateke mchokoo ambayo haitamsaidia kitu. Paulo akiwa na mshangao akauliza "U nani Wewe BWANA" naye akasikia sauti ya Yesu ikisema "Ni Mimi Yesu Ambaye wewe unaniudhi." Masikini Sauli alifikiri anafanya mema, kwa kuwafanyia ukatili watu wa Mungu kumbe anamuudhi Mungu. Hata leo ni muhimu tujiulize matendo yetu pengine hata bila kufikiria kama tunamfanyia kazi Mungu na watu Wake, kumbe tunatesa watu Wake, na kuwaletea huzuni.

Paulo aliendelea kueleza jinsi Yesu alivyomwambia ainuke, na kusimama, kwa maana alitokewa ili awe mtumishi na shahidi wa Yesu katika mambo aliyoyaona. Yesu akajidhihirisha kwake, kwa kumwokoa na kumtuma kusaidia wengine waokoke; Wayahudi na wa mataifa. Yesu akasema anamtuma afumbue macho ya mataifa na

kuwageuza waiache njia ya giza na kuelekea nuru, waache mambo ya nguvu za giza za Shetani na dhambi zao zisamehewe na wamwelekee Mungu kisha wapate wokovu na kuwa kati ya wale walioteuliwa kuwa na imani ya Yesu. Paulo akaendelea kusimulia jinsi alivyokuwa kipofu.

Kwa hiyo mfalme Agripa, sikuyaasi maono yale niliyopewa toka mbinguni, na wala sitaki kuyaasi sasa. Toka pale nimehubiri Damesiki, Yerusalemu, nchi za Uyahudi, na watu wa mataifia kwamba watubu na kubadilisha njia zao, ili waishi kwa kumwamini Mwenyezi Mungu, na Mwana Wake aliyekufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Na hii ndiyo sababu nilikamatwa hekaluni na kuburutwa nje wakitaka waniue. Basi kwa kuwa Mungu aliniahidi kwamba ataweka watu kuwa msaada wangu; ndivyo nimeweza kusimama hapa leo mbele yako, na kutoa ushuhuda kwako wa habari hii njema ya wokovu kwa wote mlio hapa. Yale niliyokwambia kuhusu Yesu wa Nazareti, ni yale Musa na manabii walitabiri, sasa yametimia. Walisema Masihi atakuja na hana budi kuteswa na kufa, na kufufuka kutoka katika wafu kwa nguvu Zake Mwenyewe.

Katika Masihi ndipo Mungu anatoa karama ya uzima wa milele kwa wote wanaoamini. Manabii pia walisema habari njema za wokovu zitaenda dunia nzima kwa Myahudi na kwa watu wa mataifa.

*Hebu wale wote wanaowatembelea Wakristo waone kwamba saa ya maombi ni ya thamani zaidi, takatifu zaidi, na ya furaha zaidi ya siku. Misimu hii ya ibada huongeza ushawishi ulio bora, safi, na wenye kuyaelekeza mawazo juu mbinguni kwa wale wote wanaoshiriki. Huleta amani na pumziko la shukrani kwa roho.
--------------------------

Maswali: Kwa nini Paulo alikuwa na ushujaa wa kusema hakuyaasi maono aliyopewa toka mbinguni? Kwa nini Sauli aliuliza u nani Wewe BWANA? Kwa nini haki ya mtu mahakamani, inaweza kupotea hata akiwa mtu ana haki?

**SIKU YA 323.**
**(Novemba 18)**

# Paulo amkatisha shauri Herode Agripa.

**Matendo 26 na 27.**

Alipokuwa akiendelea kujitetea na kushuhudia hivi, Festo akasema kwa sauti kuu "Una wazimu, kusoma kwako elimu nyingi, kumekugeuza akili." Paulo akajibu, sina wazimu, Gavana Festo, ninayokwambia si ndoto, ni Maneno ya Kweli na ya akili kamili. Maana mfalme Agripa anayajua haya nayoyazungumzia kwani ni Myahudi anayemjua Mungu toka utoto. Hii ndiyo sababu nazungumza kwako wazi wazi bila wasiwasi na kwa ujasiri nikijua sana ya kuwa hapana hata neno moja usilolijua, yote yametendeka wazi wazi.

Hakuna ambalo Yesu alilifanya vifichoni, kila mtu aliona alichofanya na kupata nafasi ya kumjua. Kwa sababu ya Yesu ndiyo maana Wayahudi walinikamata ndani ya hekalu. Paulo akamkatisha shauri mfalme Agripa kwa kumwambia "mfalme Agripa Je, waamini manabii? Najua kuwa waamini." Agripa akamwambia Paulo "wafikiri kwa maneno machache haya utanifanya mimi kuwa Mkristo." Paulo akajibu, "Namwomba Mungu kwamba ikiwa ni kwa maneno machache au ikiwa kwa mengi, si wewe tu bali hata wote walionisikia wawe kama Mimi, yaani wawe Wakristo, isipokuwa wasiwe na vifungo hivi kama mimi." Hakika wokovu ulikuwa umefika nyumbani mwake ila alikuwa anauchezea, pengine akiona kwamba ni kujiumbua. Ila maisha haya hata tuwe na cheo gani, ni cha muda mfup itu, mara nyingi watu hukaa kwenye ofisi kwa miaka michache tu, pengine 50 hivi kama mtu ni mfalme, au raisi asiyetoka madarakani. Baada ya hapo, inabidi mtu atoke. Akiendelea kuwa hapo, mara nyingi atakuwa anasukumwa kwenye baiskeli ya wasiojiweza, au kuwa kwenye kiti au kitanda kwa muda mrefu, na ratiba nyingi za matibabu. Ila milele ni muda mrefu sana, usio na hesabu, usio na mwisho! Akili zetu haziwezi kutambua hili vizuri kwasababu tuna ukomo.

Mfalme na Gavana Festo na Bernike na wale walioketi pamoja nao wakasimama, kuonyesha kusikiliza kesi kumeisha, wakaondoka wakisemezana, "Mtu huyu hajatenda lolote linalostahili kufungwa, wala kifo." Agripa akamwambia Festo, angeweza kumfungua Paulo atoke gerezani kama asingekuwa amekata rufaa kwenda kwa Kaisari Rumi. Hata hivyo ilikuwa mpango wa Mungu ashuhudie maelfu ya watu Rumi, ambao watachagua kumfuata Yesu Masihi. Hata hivyo angeachiliwa huru, wangemwua pale Yerusalemu, hasa wale watu waliolitaja Jina la Mungu wakiwa wanatumiwa na Shetani kwa ukatili na jazba huku wakafikiri wanamtumikia Mungu.

Hata leo dini nyingi zina ukatili na kuua watu wakififikiri wanamtumikia Mungu na kwamba Mungu amewaagiza waue watu. Hakuna kitu kama hicho kama mtu si mhalifu mwenye kosa la jinai. Siku hizi Mungu hana taifa Lake teule ambalo analipa ruhusa kuua watu! Ule wakati wa Israeli walipokuwa chini Yake walipewa masharti

yaliyotoka Kwake moja kwa moja, bali baada ya pale mambo yamebadilika. Paulo alikuwa amemaliza ujumbe wote wa wokovu pale, ila wadhifa wa watu unaweza kuwafanya wasiamue maamuzi ya kuwasaidia kwenda mbinguni. Hata leo tutakutana na watu wa namna hii, kwenye nyadhifa mbalimbali, wanaopata sababu za hapa na pale alimradi wasiamue kumchagua Mwenyezi Mungu, na kusoma Neno Lake kila siku na kulifuata. Wayahudi hawa walikuwa na mapokeo ya dini, ila hawakujua kinachoendelea kuhusu ufalme wa Mungu. Paulo alikaa kifungoni miaka miwili hivi. Ikawekwa tarehe ya kwenda Rumi, Paulo akapanda merekebu kwenda Italia. Aliruhusiwa kwenda na wafuasi, na watenda kazi kama Luka, Aristariko. Yawezekana na Timotheo, ila hatuna uhakika maana alikuwa Rumi, pengine kwa kumfuata baadaye.

Paulo na wafungwa wengine 276 waliwekwa kwenye mikono ya askari mmoja jina lake Yulio wa Kikosi cha Augusto. Merikebu Adramitio, iliyokuwa tayari kusafiri mpaka miji ya pwani mwa bahari ya Mediteraniani. Wakapita Sidoni, na Yulio alimtendea sana fadhila Paulo, akijua ni mtumishi wa Mungu. Kisha wakapita Kupro, badala ya kwenda moja kwa moja maana upepo ulikuwa mkali.Paulo alipata nafasi ya kuonana na waumini, na hata kushuhudia katika safari ya kwenda Rumi, kwani safari ilichukua miezi mitatu. Kutoka pale walienda Kilikia mji aliozaliwa na kisha Pamfilia, na kufika Mira kule Likia. Pale akida au askari Yulio alikuta Meli toka Iskanderia, Misri tayari kusafiri kwenda Italia.

Akawapandisha wale watu 276 humo, na wakasafiri pole pole kwa muda wa siku nyingi, mpaka kufika Nido kwa shida kwasababu upepo uliwazuia, wakapitia chini kisiwa cha Krete, kuikabili Salmone. Wakapita kwa shida na kufika mahali panapoitwa bandari nzuri karibu na mji uitwao Lasea. Hapa walitumia muda mwingi bila sababu ya maana. Wale viongozi walipokuwa tayari kwenda magharibi Italia, ilikuwa wakati wa hatari umefika, kwani ikipita siku ya Wayahudi ya upatanisho ni miezi migumu ya kusafiri kwa meli, kwa sababu dhoruba za baridi na theluji zinaleta shida.

Paulo aliwaonya kwa kuwaambia “wanaume, naona sasa, safari hii itakuwa ya madhara na hasara nyingi kwa shehena, merikebu na maisha yetu pia, maana ni miezi ya pepo na dhrouba kali.” Yulio aliyekuwa askari kiongozi, asitake kumsikia Paulo, maana alikuwa mtu wa kawaida, asiye na ujuzi. Badala yake alimsikiliza nahodha mwenye meli, aliyetaka kuendelea na biashara yake au mradi wake, basi waliamua kwenda. Manahodha na abiria pia waliona bandari nzuri na ndogo wakaamua kukaa wakingoja miezi ya baridi na theluji iishe. Wakawa tayari kuhatarisha maisha yao ili waende Foinike, karibu na Krete kwenye bandari na mahali pazuri zaidi. “Upepo ukaja, na wale watu wakaona wamepata kitu walichotaka na wakang’oa nanga na kwenda pwani ya Krete.

*Maombi ya Kila Siku ya Kupaa kwa MUNGU kama Uvumba Mtamu—Maisha ya Abrahamu, rafiki ya MUNGU, yalikuwa maisha ya maombi. Kila mahali alipopiga hema lake, karibu na nalo ilijengwa madhabahu, ambayo juu yake ilitolewa sadaka ya asubuhi na ya jioni. Wakati hema lake lilipoondolewa, madhabahu ilibaki. Na Mkanaani anarandaranda huko, alipofika kwenye madhabahu hiyo, alijua ni

nani aliyekuwepo hapo. Naye alipopiga hema lake alitengeneza madhabahu na kumwabudu MUNGU aliye hai.

-----------------------------

Maswali: Festo na mfalme Agripa II walipataje nafasi ya kumjua Mungu? Kwa nini Yulio hakumsikiliza Paulo? Kwa nini walisema hawawezi kumwachilia huru Paulo? Kwa nini watu wakishuhudia Neno la Mungu mara zingine huambiwa wana wazimu? Hebu jadili na wenzako kuhusu yale majukumu waliyopewa serikali ya Israeli wakati wa Joshua na ukilinganisha na serikali ya Israeli leo!

**SIKU YA 324.**
**(Novemba 19)**

# Kuvunjikiwa merikebu na kuogelea.

**Matendo 27.**



Safari siku hizo ilikuwa na shida nyingi. Vyombo vilikuwa si imara, havikuwa na injini, na walitumainia nyota na jua kusafiri na dhoruba zilikuwa kali. Hata hivyo yote yalitokea kwa ubinadamu wa yule akida kumsikiliza nahodha wa meli, kuliko mtumishi wa Mungu. Ni kweli kibinadamu nahodha ndiye alijua kinachoendelea kuliko Paulo, ila Paulo alikuwa anaongozwa na Roho wa Mungu. Paulo alikuwa mtu mzima pengine alifikisha miaka sitini na marafiki zake kama vile Luka na Aristariko waliamua wamsindikize mtu wa Mungu.

Mabaharia walikuja kugundua baadaye Paulo ni nani, kweli asiyekujua hakuthamini. Nasi katika maisha yetu tujihadhari kusikia ushauri wa watu fulani, marafiki na watalaamu kuliko Mungu. Basi wakienda pwani ya Krete, baada ya muda si mchache upepo uitwao Eurakilo, ukavuma kwa nguvu, kama tufani. Huu ulipiga merikebu vibaya, isiweze kushindana na upepo, ikachukuliwa na kupita kisiwa kidogo kiitwacho Kauda, wakajaribu kuweka mashua ya kuokoa watu. Mashua ya kuokoa watu iliyokuwa ndani ya merikebu ilikuwa imefungwa kwenye merikebu (lifeboat).

Wakatumia misaada kuikweza, wakaikaza merikebu kwa kupitisha kamba chini yake wakiogopa wasije wakakwama. Wakatua nanga wakiogopa upepo utawapeleka kwenye mchanga kwenye pwani ya Kirene Libya. Hata hivyo walichukuliwa, maana walipigwa sana na tufani, na siku ya pili yake walianza kutupa shehena baharini. Siku ya tatu wakatupa vyombo vya merikebu kwa mikono yao wenyewe. Jua wala nyota hazikuonekana kwa maana ukungu ulitanda na dhoruba kwa siku nyingi, na ile tufani ilimkatisha kila mtu tamaa ya kuokoka.

Wakiwa wamekaa wakati mwingi bila kula chakula vizuri, Paulo alisimama na kuwaita abiria na watu akisema kwa sauti ya juu ili asikike katika dhoruba ile "wanaume mngenisikiliza yale niliyowaambia msitoke kule bandari nzuri kwenye pwani ya Krete, msingepata hasara na madhara haya. Sasa nawapeni ushauri, iweni na moyo mkuu, kwa maana hapana hata nafsi moja miongoni mwenu itakayoangamia, japo merikebu itaangamia. Jana usiku Malaika wa Mungu wa mbinguni ambaye mimi namtumika, alisimama karibu yangu na kusema "Paulo usiogope, maana huna budi kusimama mbele ya Kaisari. Tena Mungu amesikia mambo yako na amekupa wote wanaosafiri pamoja nawe. Wote wataokoka na pia utapata nafasi ya kuwasimulia kisa cha wokovu. Basi wanaume, changamkeni; kwa sababu namwamini Mungu alichosema kitakuwa vile vile alivyoniambia. Ila mara hii merikebu yetu itavunjika na tutapwelea kwenye kisiwa kimoja si mbali na hapa" Siku ya kumi na nne ilipofika, walichukuliwa katika bahari ya Adriatic, kama usiku wa manane, baharia wakadhani wanakaribia nchi kavu. Na kumbe wapo km 700 toka nchi kavu. Wakatupa bildi au kamba wakaona kwamba kina ni futi 120. Baada ya masaa machache wakatupa tena wakakuta kina cha maji ni futi 90. Wakatupa tena wakakuta kina futi 15, wakaogopa wasije wakajitosa na kujigonga kwenye miamba. Wakatua nanga nene wakaomba kuche maana ilikuwa usiku. Usiku ule manahodha wengine walitaka kutoroka waiache merikebu. Waliweka mashua ya kuokoa watu waende nayo, huku wakijidai wanatupa nanga. Paulo alipowaona alimtahadharisha Yulio, akisema "hawa wasipokaa merikebuni hamtaweza kuokoka" basi askari walizikata kamba za mashua ya kuokoa watu ili iende zake.

Kulipopambazuka, Paulo aliwasihi watu wote wale chakula, maana ni siku ya kumi na nne, hawajala vizuri, ni kama wamefunga, akawasihi wale chakula maana itakuwa wokovu kwao, ili waokoke, "wala msiwe na hofu maana hapana hata unywele mmoja wa vichwa vyenu utakaopotea." Aliposema vile alitwaa mkate na akamshukuru Mungu mbele yao, kisha akaumega na kuanza kula. Ndipo wote walipochangamka na kwa faraja hiyo wakaanza kula. Kila mtu alipokwisha kula na kushiba, walipunguza shehena ya merikebu.

Kulipoanza kucha hawakuitambua ile nchi, ila waliona ufuko kama ni mahali salama pa kuweka merikebu yao. Manahodha wakazitupa nanga zao baharini na kuzilegeza kamba za usukani na kuleta tangi dogo ili liushike upepo ili waunde ufuko. Ila walifika mahali bahari mbili zinapokutana. Mahali ambapo maji hayakuwa mengi, walipoegesha merikebu yao, na hapo waligonga mchanga kwa nguvu na merikebu ikakataa kutoka na pepo kali zikaanza kuvunja merikebu vipande vipande. Shauri la askari ilikuwa kuwaua wafungwa ili mtu asiogelee na kukimbilia nchi kavu. Akida Yulio, akimpenda Paulo na kutaka kumponya mtu wa Mungu aliwazuia wasifanye ukatili ule. Akawaamuru wale wawezao kuogolea wajitupe kwanza baharini, wafike nchi kavu, nao waliosalia wachukue mbao na vitu vingine waelelee wakienda kwenye pwani. Hivyo watu wote waliokolewa na kufika nchi kavu salama. Watu hawa walikuwa na baraka ya pekee ya kusafiri na watu wa Mungu. Usalama ukapatikana kwao kwa ajili ya watu hawa. Hata leo ukijiweka na watu wanaomwabudu Mungu wa Kweli wa mbinguni, wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, na kufuata njia Zake na Neno Lake kwa makini utaokolewa. Pengine wengi kati ya wale 276 walimwamini Mungu njiani kwa ile miezi mitatu. Siku hizi safari kama

hiyo yawezekana kufanyika kwa siku mbili hivi.

*Enyi akina baba na akina mama, kila asubuhi na jioni wakusanyeni watoto wenu karibu nanyi, na kwa dua ya unyenyekevu inueni moyo kwa MUNGU kwa ajili ya msaada. Wapendwa wenu wanakabiliwa na majaribu. Kero za kila siku zinasonga njia ya vijana na wazee. Wale ambao wanahitaji kuishi maisha ya uvumilivu, ya upendo, na uchangamfu lazima wasali. Ni kwa kupokea msaada wa kila wakati kutoka kwa MUNGU tunaweza kupata ushindi juu ya nafsi yetu.
---------------------

Maswali: Paulo aliwatiaje moyo wasafiri? Mungu alimtia moyo Paulo kwa maneno gani? Watu wangapi waliokoka kwenye ile merikebu? Ni Njama gani manahodha walizofanya ambazo Paulo alimwambia Yulio? Kwa nini askari hawakuwaua wafungwa?

**SIKU YA 325.**
**(Novemba 20)**

# Kisiwani malta na ukarimu wao.

**Matendo 28**



Walipokwisha kuokoka ufukoni waligundua wako kwenye kisiwa cha Malta (kiangalie kwenye ramani), ni sehemu ya Afrika. Watu hawa leo wanazungumza Kiarabu ila wanakiandika kwa alfabeti kama zetu yaani za kilatini, na wala si za kiarabu. Wenyeji wa hapa walikuwa si watu wa elimu nyingi au wenye maendeleo, (washamba primitive), bali walikuwa ni watu wakarimu, na wakawafanyia fadhili zisizokuwa za kawaida. Mungu hahitaji watu wa elimu nyingi bali wenye upendo ambao japo hawamjui kwa kina wanatimiza Sheria Yake kutokana na ufahamu wao wakiwa wamejaa matendo mema kama kitabu cha Warumi kinavyosema. Wakati huu wa baridi, wakiwaona na nguo mbichi kwa kuogelea na mvua, waliwasha moto, ili waote na kuwakaribisha.

Wakikusanya kuni, Paulo alileta mzigo wa kuni, na kuuweka motoni, hapo ndipo nyoka wa sumu akatoka kwenye ule mzigo wake na kumwuma kisha akamzonga zonga mkononi mwake. Wenyeji wa Malta walipoona vile walisema "hakosi mfungwa huyu anashitakiwa kwa mauaji, maana japo ameokoka kutoka kwa dhoruba ya bahari, haki haimwachi kuishi, maana uovu wake ni mwingi." Paulo alimkung'uta

yule nyoka akaangukia motoni asipate madhara yoyote. Wao wakadhani atavimba na kuanguka chini afe, kwa kutambua sumu ya yule nyoka ilivyo. Ila hakuna kilichotokea, alikuwa mzima wa afya. Baada ya kumwangalia sana, na kuona hakuna dhara linampata waligeuka na kusema yeye ni mungu. Binadamu asiyemweka Mungu mbele ni rahisi sana kuabudu miungu mingine kwa kila kitu anachotekewa nacho.

Si mbali na pale kulikuwa na mashamba ya mkuu wa kisiwa jina lake ni Publio. Tajiri huyu mkarimu, aliposikia, aliwakaribisha wale waliovunjikiwa na merikebu. Paulo na marafiki zake wainjilisti walienda na wakafanyiwa ugeni wa heshima. Walikaribishwa kwa moyo wa ukarimu na urafiki kwa siku tatu. Baba wa Publio alikuwa mgonjwa mahututi wa homa na kuhara damu, alikuwa kitandani hajiwezi. Paulo akaomba amwone, akaweka mkono wake juu ya kichwa cha baba Publio, akimwombea naye akapona. Habari hizi zikaenea kwa upesi kisiwani kote na watu wengi wakaja na wagonjwa wao katika kisiwa kile na wote Paulo aliwaponya kupitia nguvu za Mwenyezi Mungu.

Watu wa Malta walibarikiwa na timu ya wainjilisti wale. Wakapewa heshima kubwa na watu na siku walipotoka walipewa zawadi nyingi, na mahitaji yale waliyokuwa nayo yalikidhiwa. Ndipo walipoingia melini pamoja na vitu vyao. Baada ya miezi mitatu kisiwani, naamini wengi walimpokea Yesu hapa, na kumkubali Mungu wa Kweli aliyeumba mbingu na dunia na vyote vilivyomo. Walipanda Merikebu ya Iskanderia iliyokuwa imekaa pale kisiwani, wakati wa baridi, hii ilikuwa na alama ya ndugu pacha, miungu ya Kirumi iitwayo Casto na Poluksi.

Kutoka hapo walizunguka kwa mguu kwa kilomita 150 hivi na kufika kule Syracuse, kisha Regio na baada ya siku tatu upepo ulivuma na siku ya pili walifika Puteoli, karibu na mji wa Naples Italia. Huko walikuta ndugu waumini wa Kikristo wamejitayarisha kuwapokea na wakawasihi wakae nao siku saba, kisha merikebu ikafika Rumi. Baada ya haya yote, manahodha na hata askari walikuwa wamefanya urafiki mzuri hata kukaa mahali siku saba. Mfungwa Paulo akaomba na kuhubiri akiimarisha washiriki pale.

Paulo alikuwa mhudumu shujaa wa Kristo, hakuchoka kushuhudia, na wenzake aliokuwa nao. Luka na Aristariko walifanya kazi kisiwani bila kuchoka. Mfano huu ni wa kufuatwa nasi sote, tunaomwamini Yesu. Kama unataka kujenga tabia bora na njema lazima kufuata tabia hii ya mhubiri huyu wa injili. Paulo alisafiri safari kama nne ndefu hivi, waweza kuangalia ramani zake kwa undani kwenye tovuti. Ombea wale unaoshiriki nao injili. Mwombe Mungu awape moyo wa kupenda kupokea Maneno Yake. Sehemu yako ni kuwa mwaminifu kuongea nao. Yesu alituachia agizo akisema "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Amina". Ahadi ya ajabu iliyoje! Ina Mamlaka yote toka Kwake, na kisha atakuwa nasi mpaka mwisho wa dunia!

Hebu na tuombe ujasiri kama wa Paulo! Aliwafanya wengi wamwamini Masihi ikiwemo nyumba ya mtawala wa Himaya aliyeitwa Nero. Huwezi kusoma kwa kisa cha Paulo na usiamini kwamba alisadiki kwa moyo wake wote kwamba Yesu Ndiye njia, Kweli, na uzima. Alikuwa na uhakika wa kile alichokiamini naye akawa tayari kufa kwa ajili ya imani yake. Adui mkubwa wa Yesu, sasa akawa anampenda sana Yesu kwa sababu Yesu aliyefufuka alimtokea na kuondoa ujinga wake (kutojua). Ni wale tu walio na imani ya aina hii ndiyo ambao watafanikiwa kupitia ule wakati wa taabu ya Yakobo unaonenwa na nabii Yeremia. Hebu tumwombe Mungu atupe imani hii.

*Kila asubuhi jiweke wakfu kwa MUNGU na watoto wako kwa siku hiyo. Usifanye hesabu kwa miezi au miaka; hiyo si yako. Umepewa siku moja fupi. Kana kwamba ndiyo mwisho wako duniani, fanya kazi kwa Mwalimu wakati wa saa zake. Weka mipango yako yote mbele za MUNGU, itekelezwe au kutolewa, kama vile uelekezaji Wake utakavyoonyesha. Kubali mipango Yake badala ya mipango yako mwenyewe, ingawa kukubali kwake kunahitaji kuachwa kwa miradi inayopendwa. Hivyo maisha yatafinyangwa zaidi na zaidi kufuatana na mfano wa kimungu; "Na amani ya MUNGU, ipitayo akili zote, itahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu." Wafilipi 4:7 .

--------------------------

Maswali: Malta ipo wapi kwenye ramani? Je, lugha ya Malta inafanana na lugha gani? Paulo alipoumwa na nyoka watu walisemaje? Publio alikuwa nani? Watu wa Malta walibarikiwa na wainjilisti au watumishi wa Mungu? Mji gani Paulo alichukuliwa kifungoni? Naples ipo nchi gani? Je, unazungumza na majirani zako kuhusu Masihi?

**SIKU YA 326.**
**(Novemba 21)**

# Paulo ashuhudia Rumi na kuandika barua kwa makanisa.

**Matendo 28.**



Ndugu Wayahudi walipopata habari Paulo anaingia Rumi na wainjilisti Aristariko na Luka tabibu mpendwa, walikuja kuwalaki mahali paitwapo soko la Apio, na mikahawa mitatu kama kilomita 60 hivi toka mjini Rumi. Yulio aliwapeleka wale wafungwa kwa askari na gereza la Kaisaria Rumi. Ila walimtendea Paulo kwa heshima kwa sababu ya sehemu aliyofanya kwenye kuharibikiwa meli. Yulio aliwaeleza haya na Paulo akapewa nafasi ya kuwa na mahali pake binafsi na askari aliyemlinda. Aliruhusiwa marafiki wamtembelee. Alipenda siku moja afike Rumi kuhubiri hata alikuwa ameshawaandikia barua ya ajabu kuhusu Kisa cha msalaba, na sasa alifika Rumi na kuikanyaga ardhi yake. Hii ilimpa faraja na ujasiri hivyo Paulo akamshukuru Mungu kwa upendo wa ndugu na kujali kwao japo alikuwa kwenye pingu akihesabiwa kama mhalifu, hawakumwonea aibu.

Waumini waliomjua Paulo walijua fika kwamba Mungu anamtumia kama chombo kiteule ili wengi wapate uzima wa milele. Paulo alijieleza kwa ndugu na waumini hawa akieleza kisa chake na kushuhudia. Shujaa Paulo huyu ameleta mamilioni kwa Kristo kwa kazi na Maandishi Yake. Japo kisomo si cheti cha kumfanyia kazi Mungu ila kwa yule aliyesoma vizuri atafikia watu wa aina fulani kirahisi na ataweza kupata nafasi ya kuweka vitu kwenye mandishi na kuzungumza na watu wenye wadhifa. Kila binadamu amepewa uwezo wa kufikia watu wa aina fulani ambao mtu mwingine hawezi kuwafikia, wazungu wanaita kufikia kwenye mizizi ya majani 'grassroot'.

Baada ya siku tatu Paulo aliwaita wakuu wa Wayahudi walio Rumi wakutane naye akawaelezea yaliyompata. Aliwaambia pengine wamesikia jambo kuhusu habari yake, ila yeye, hakufanya kitu kinyume cha dini ya Kiyahudi ya baba zao, ila alitiwa gerezani Yerusalemu katika mikono ya Warumi na gavana alipochunguza mambo alikuta hana hatia na mashitaka waliyoleta Wayahudi, na alipanga amwache huru, kwa kuwa hakuwa na hatia ya kufanya auwawe. Ila Wayahudi walipokataa awe

huru, “na nikaona Gavana anaweza kunitia mikononi mwa Wayahudi, nikakata rufaa nimwone Kaisari, japo wale walionifanyia ubaya ni wale wa taifa langu nyumbani.”

“Sina kinyongo nao, na wala sina mpango wa kusema lolote baya dhidi yao, na ndiyo maana nimewaita hapa kusudi niwaeleze ni kwa nini nipo vifungoni hivi. Nimo vifungoni kutokana na imani yangu kuhusu Masihi na tumaini la Israeli.” Wale waumini wa Rumi walimwambia wao hawakupata habari yoyote kwa nyaraka kuhusu habari zake, kutoka Uyahudi wala pale Rumi na hakuna ndugu hata mmoja aliyefika na kuwapasha habari hizo au kunena lolote baya lihusulo Paulo. Wakamwambia wangependa kusikia kutoka kwake vile yeye aonavyo. Kwa kuwa madhehebu hayo ya Kikristo yamejulikana kwao, lakini yanazungumzwa kila mahali kwa namna mbaya.

Waliagana naye na wakamjia katika nyumba aliyokaa, watu wengi sana. Akawaeleza kwa taratibu na kuwashuhudia ufalme wa Mungu, kuanzia asubuhi mpaka jioni. Aliwaonyesha maana ya ufalme wa Mungu inavyosemekana katika Maandiko. Aliendelea kuwaonyesha unabii wa Yesu Masihi kutokana na vitabu vya Musa na manabii, kwamba Ndiye Yule aliyetarajiwa. Wengine alipomalizana nao, walikubaliana kumwamini Yesu Masihi, ila wengine walibishana wenyewe kwa wenyewe.

Paulo aliwaambia kabla hawajaondoka, kwamba Roho Mtakatifu alizungumza kupitia nabii Isaya hayo, kwa mababa zao nyuma akisema “Enenda kwa watu hawa, ukawaambie, kusikia mtasikia wala hamtafahamu; Na kuona, mtaona wala hamtatambua; Kwa maana mioyo ya watu hawa imepumbaa. Na masikio yao ni mazito kusikia, Na macho yao wameyafumba; wasije wakaona kwa macho yao, na kusikia kwa masikio yao, na kufahamu kwa mioyo yao, na kubadili nia zao, nikawaponya.”

Paulo aliwaambia anategemea kwamba wanajua wokovu ni wa kila taifa lugha na jamaa. “Kama ninyi Wayahudi msipoamini au mkiamini kuna wengi wa mataifa wako tayari.” Wayahudi hawa wengi hawakusiliza kile Paulo alichosema nao wakatabasamu na kumwambia kwaheri wakitoka mlangoni na kuendelea kubishana wao kwa wao. Walikuwa watu wema tu, hawakumfanyia ubaya mtumishi wa Mungu, bali walifanya mioyo kuwa migumu wasimpokee Yesu wakiogopa maisha yao yatabadilishwa. Walipenda kubaki vile vile. Hawakutaka kujisalimisha kwa Mungu au kujitoa kwa Yesu. Je, wewe upo tayari kujisalimisha kwa Yesu au unataka kubaki vile vile, ukisikia kisa hiki cha thamani, na usiseme kwa watu wa Mungu, ‘nipe habari za Yesu, kwangu ni tamu sana’, na kisha hukati shauri kwa upendo huu wa Yesu wa thamani.

Paulo aliendelea na kushuhudia habari njema za injili. Agripa na wenzake ambao hawakuwa na haraka ya kesi wakijua Paulo si mhalifu, na wakitaka kuchukua muda kutunga mengine ya hila walichukua muda kufika. Kwa miaka miwili, alibaki kwenye kizuizi cha nyumbani akiwa chini ya ulinzi. Akaendelea kuzungumzia ufalme wa Mungu kwa ujasiri mkuu, akikomboa wakati maana alijua siku zake

za kuuwawa zi karibu. Alifanya hili wazi wazi na hakuna aliyemzuia asishuhudie habari njema. Aliwaambia hata wale wa nyumbani mwa Kaisaria na maaskari pia wengi wakaamini (Tazama Wafilipi 1:12 na Wafilipi 4:22).

Paulo alipata nafasi baadaye ya kusafiri tena, na kisha akarudi kifungoni na kuandikia makanisa machanga mengine aliyoanzisha yeye au wanafunzi wengine. Barua hizi zinaitwa barua za kifungoni, nazo ni kama Wafilipi, Timotheo, Wakolosai, Waefeso, na Filemoni. Aliwapa faraja na kuwahimiza, kwa mambo mengi. Barua hizi zilikuwa ndefu. Akimalizia aliandika, "Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda, baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo BWANA mhukumu wa haki, atanipa siku ile, wala si mimi tu, bali na watu wote pia wanaopenda kufunuliwa Kwake." Yasemekana Paulo aliuwawa na mfalme Nero mwaka 68 BK.

Paulo na mitume walijitahidi kuwasaidia Wayahudi na watu wengine kuondoa ubaguzi wa makabila na dini. Aliwaeleza kuhusu habari za Masihi Yesu Ambaye alikuwa ameshafika, na kufa na kufufuka na wengi walijua habari hii ni ya Kweli ila wasikate shauri. Walihimiza ni bora kupata mateso kwa kufanya mema kuliko uovu. Paulo na mitume walikuwa wahudumu bora wa Mungu. Walifanya kazi bila kuchoka, kumshuhudia Mungu. Hari na kujitoa kwao kwa Mungu kwahitaji kuungwa mkono nasi wote tunaomwamini Yesu Mwana wa Mungu. Kama tunataka kuwa na tabia nzuri, lazima tutilie maanani vile vitu mitume walifanya na kuvithamini. Hebu na tufuate nyayo zao.

*Mambo ya Kuombea Kila Siku—Tunapaswa kulitazama kila jukumu kuwa takatifu kwasababu ni sehemu ya utumishi wa Mungu, hata jukumu hilo liwe la unyenyekevu wa kiasi gani. Ombi letu la kila siku linapaswa kuwa , "Bwana, nisaidie kufanya vizuri kwa uwezo wangu wote. Nifundishe jinsi ya kufanya kazi bora. Nipe nguvu na uchangamfu. Nisaidie kuleta katika huduma yangu huduma ya upendo ya Mwokozi. "
----------------------------

Maswali: Paulo alifika Rumi na watenda kazi gani wengine? Yulio alifanya nini walipofika Rumi? Paulo aliwekwa kwenye kifungo cha aina gani? Kwa nini Paulo alikata rufaa ya kumwona Kaisari? Kwa nini watu hawakutaka kubadilika Paulo alipozungumza nao? Je, wewe u tayari kubadilika na kujisalimisha kwa Mungu 100%? Watu wasiomjua Paulo walifikiriaje wakiona mzee anapita akiwa na pingu wakiandamana na wafungwa wengine? Je, umeshawahi kuambiwa habari za Kweli na za muhimu ila usikate shauri?

**SIKU YA 327**
**(Novemba 22)**

# Barua za Paulo, Mitume na Yuda na Yakobo.



Paulo akiwa Rumi kama mfungwa alipata nafasi ya kuhubiri injili, na kutembelewa na marafiki na kuandika barua kwa makanisa aliyosaidia kuanzisha. Luka, Aristariko, Marko, Timotheo na wengine waliendelea kuhudumu naye. Barua tulizo nazo ni baadhi tu ya zile zilizo kwenye Biblia. Agano Jipya lina barua 21, zilizoandikwa kwa makanisa yaliyoanzishwa, baada ya kufundishwa habari za Masihi. Yasemekana barua hizi ziliandikwa hata kabla ya vitabu vya injili kuandikwa. Kati ya hizi 14 ni barua za Paulo ikiwemo ile ya Waebrania. Barua za Paulo ni zaidi ya nusu ya Agano Jipya. Nashauri wazazi wajadili na watoto wao barua hizi, na kukariri mafungu toka barua hizi. Tusingependa kuziruka barua hizi maana zina mafundisho mengi mazuri sana na ni sehemu ya Maandiko Matakatifu. Paulo alikuwa mwandishi mashuhuri wa barua, kwani barua hizi zinasomwa na mamilioni ya watu mpaka leo. Yasemekana Wagalatia na Wathesalonike, ndizo barua za kwanza kuandikwa kwenye 45 BK.

Paulo alikuwa Mfarisayo, Myahudi wa kabila la Benyamini. Kwanza aliitwa Sauli, na alikuwa na uraia wa Rumi maana alizaliwa Kilikia, Tarso. Alijifunza chini ya

Rabi Gamalieli, Yerusalemu. Aliandika barua kwa makanisa mapya yaliyoanzishwa kuwatia moyo kuhusu mahusiano yao na Mungu, mahusiano yao na watu na mahusiano yao na familia zao. Katika barua zake alizungumza na watu mbali mbali na hivyo aliandikia watu kutokana na utamaduni wao. Alisema kwamba yeye japo yu huru amejifanya mtumwa kwa wote, kwa Wayahudi akawa Myahudi ili awafikie Wayahudi, kwa wale ambao wako chini ya sheria alikuwa naye chini ya Sheria ili awafikie, na kwa wale wanyonge alikuwa mnyonge ili awafikie wanyonge. Yaonyesha kwamba hakuoa, kwa ajili ya kutaka kumfanyia kazi Mungu.

Japo yawezekana siku za nyuma akiwa mjumbe wa baraza la Sanhedrin alikuwa na mke ila hapo mbeleni huenda kwa kufiwa mke akawa mgane. Alijipatia riziki kwa ustadi wa kutengeneza mahema. Alipenda kuridhika na kutotegemea watu "alijua kudhiliwa, tena kufanikiwa katika hali yote na katika mambo yote alifundishwa kuona njaa na kuwa na vingi, na kupungukiwa." Alijua anayaweza mambo yote Kwake Mungu amtiaye nguvu. Alichukuliwa kwenda Uarabuni kufundishwa miaka mitatu na Roho Mtakatifu. Alikuwa mtu mnyenyekevu hata kujiita "mkuu wa wenye dhambi." Alihubiri, na kuponya akitumia nguvu za Mwenyezi Mungu. Alifanya kazi na wengi kama vile Baranaba, Mwana wa matumaini, Sila, Marko, Timotheo, Prisila, Akila, Tabibu Luka na wengineo. Pamoja na mafundisho makuu ya imani barua hizi zinatusaidia kujua Historia ya kazi ya Mungu ilivyoendelea, na kuanza kwa kanisa la Kikristo.

Japo Warumi imeorodheshwa kama barua ya kwanza ya Paulo aliandika barua hizi kwa mtiririko au mpangilio huu Wathesalonike, Wagalatia, Wakorintho, Warumi, Wakolosai, Waefeso, Wafilipi, Filemoni, Timotheo wa kwanza, Tito, Timotheo wa pili. Barua nyingi ziliandikwa kuanzia mwaka wa 45 BK mpaka 65 BK. Epafradito na Timotheo walichukua barua ya Paulo kwenda Filipi, barua hiyo iliyojaa maneno mengi ya faraja, furaha upole na uungwana. Onesimo alichukua barua kwenda kanisa la Kolosai. Barua ya Kolosai haikushugulika na shida iliyotokea bali mashauri ya Kikristo. Barua hizi zilikuwa na ujumbe wa upendo mwingi, maana mitume waliwaandikia watoto wao katika imani. Mitume waliwatabikia waumini hawa wachanga, kuwapa ushauri katika kila nyanja za maisha, ili wasipungukiwe na karama ili wamtumikie Kristo mpaka kuja Kwake mara ya pili.

Mitume walitaka waumini wawe waaminifu mpaka siku ile Yesu atakapoonekana mawinguni, wakiishi maisha ya utauwa, upole, utulivu, upendo, amani, furaha, tumaini na uvumilivu. Nyaraka au barua hizi ziliwakumbusha kwamba watakuwa na matatizo kwani adui anataka waanguke na kuumia, ila wasiwe na shida, maana hakuna kitu kitawatenga na upendo wa Kristo, iwe dhiki, mateso, njaa, kukosa nguo, upanga au shida yoyote. Pengine ukisoma barua za Paulo, kuna mambo ambayo unapata shida kuyaelewa, kwa kirahisi. Usitindikiwe, kwani hata Mtume Petro alisema "kuna baadhi ya mambo ambayo barua za ndugu yetu Paulo, zinakuwa ngumu kueleweka." Ukisoma kumbuka kwamba barua hizi ziliandikwa kwa nani, kipindi cha kuandikwa na matatizo yaliyokuwepo kwa waumini hao.

Wakristo wengi walikuwa wametoka kwenye maisha ya kuabudu miungu mingine yaani imani za kipagani na walihitaji kufundishwa ile Kweli. Hii ilihitaji umakini

na upendo ambao mtume Paulo alikuwa nao. Paulo alimtumikia BWANA kwa moyo wake wote na nguvu zake zote, akijua yule aliyemwamini na kusadiki ya kwamba anaweza kukilinda kile kilichowekewa amana kwake hata siku za mwisho. Akimwandikia Timotheo alimwambia "lihubiri Neno, uwe tayari wakati ukufaao, na wakati usiokufaa. Karipia, kemea onya, kwa uvumilivu." Alijua kuna wakati ambao watu watayakataa mafundisho ya uzima na kuzifuata njia zao wenyewe, wakijipatia walimu makundi makundi, na kuzigeukia hadithi za uongo. Akamwambia Timotheo awe na kiasi katika mambo yote, avumilie mabaya na kufanya kazi ya mhubiri wa injili akitimiza huduma. BWANA alimpa Paulo nguvu ili watu waokolewe kutoka kinywa cha simba yaani Ibilisi.

Wengine walioandika barua katika Agano Jipya ni Yuda, Ndugu wa Yesu, Yakobo ndugu wa Yesu, Yohana na Petro ambao walikuwa mitume. Paulo alikuwa huru kuendelea kumshuhudia Kristo, yasemekana wakati fulani alipewa muda wa kuwa huru kutoka kifungoni na kusafiri, kisha alirudi Rumi tena. Hapo ndiyo aliuwawa na mtawala Kaisaria Nero. Maneno yake ya mwisho kama tulivyosema yalikuwa ya kutia moyo "Nimevipiga vita vizuri, imani nimeilinda, mwendo nimeumaliza, nangoja taji niliyowekewa, na si mimi tu bali kila anayempenda BWANA." Hebu nasi tuweze kuishi maisha yatakayoakisi Maneno haya.

*Jiweke wakfu kwa MUNGU asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako liwe, "Nitwae, Ee Bwana, niwe Wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni pako. Nitumie leo katika huduma Yako. Kaa nami, na kazi yangu yote ifanyike ndani Yako." Hili ni mada na suala la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Mkabidhi Yeye mipango yako yote, ili itekelezwe au isitelekezwe kulingana na atakavyoongoza. Kwa hivyo siku baada ya siku unayakabidhi maisha yako mikononi Mwake Mungu, na hivyo maisha yako yataundwa/yatafinyangwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo.
-----------------------------

Maswali: Paulo na mitume waliandika barua kwa makusudi gani? Je, unaandikia marafiki zako na kuwashuhudia kuhusu habari za Mwenyezi Mungu? Paulo alimpa mafundisho gani Timotheo? Watu gani wengine walioandika barua kwenye Agano Jipya?

**SIKU YA 328**
**(Novemba 23)**

# Warumi. Tunaokolewa kwa Imani, kupitia Yesu tu! Si kwa matendo ya sheria.

# Nami siionei haya injili!



Watu wengi wameita kitabu hiki "kitabu cha injili kilicho wazi kupita vyote. Paulo aliandika barua ya Warumi mwaka wa 60 BK hivi, akiwa Korintho mji wa Uyunani. Alikuwa hajawahi kufika Rumi, ila alijua kuna wafuasi kule ambao walianza kukutana waliposikia habari za kufa na kufufuka kwa Yesu Masihi, aliyeahidiwa. Rumi ilikuwa na mkusanyiko wa watu kutoka kila mahali duniani, maana ndio yalikuwa makao makuu ya himaya ya Rumi. Walikuwa na miziki, michezo ya ushindani, burudani, na hata michezo ya kikatili ambayo kutokana nayo watu walikufa. Michezo ya watu kutupwa kwenye wanyama wakali na watu wakifurahia jinsi alivyoraruliwa akijaribu kujihami ni mifano ya michezo hiyo.

Mji huu ulikuwa na wengi pia wanaompenda Mungu kama Prisila na Akila, Foebe na wengine wanaotajwa kwa kusalimiwa kwenye sura ya 16. Paulo alitembea umbali mkubwa pengine kuliko wengi wa wamishionari wa siku zile, ambapo kulikuwa hamna magari, ndege, simu, barua pepe, whatsap au treni. Mawasiliano yalikuwa magumu, hivyo barua zake kama ile ya Warumi zilisaidia wengi. Paulo aliwaombea Warumi bila kukoma, nasi tuwaombee wazazi wetu, ndugu zetu na watu wote wasiomjua Kristo. Paulo anawaambia waumini kwamba kwa kupitia imani katika Yesu na kile alichokifanya kwa ajili yetu; yaani kufa kwa ajili yetu, tunapatanishwa na Mungu. Hii ina maana tuishi maisha yetu kwa ajili Yake.

Warumi 1:1 inasema "Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa aihubiri Injili ya Mungu" Sisi je, tumetenganishwa na nini leo? Roho Mtakatifu alijua kwamba sote tunahitaji ujumbe wa Warumi. Anaelezea tatizo kubwa zaidi katika historia ya mwanadamu-hukumu ya Mungu kwa wanadamu

kama matokeo ya ukosefu wetu wa haki na kujihesabia haki wenyewe. Suluhu ya kibinadamu kwa tatizo la hatia na kutengwa na Mungu daima limekuwa jambo zito kwetu binadamu -kwani kwa juhudi zetu hatuwezi kulipa ufumbuzi unaotakiwa. Mifumo ya kidini iliyobuniwa na mwanadamu haiwezi kuziba pengo. Tunaona "Wayahudi na Wasio Wayahudi wote wako chini ya nguvu ya dhambi" ( 3:9 ), tatizo hilo ni kubwa sana hivi kwamba ni Mungu pekee awezaye kulitatua. Basi tunahitaji kuvuliwa haki yetu wenyewe ili tukimbilie kwa Kristo na dhabihu Yake kama haki yetu pekee. Kisha, tukihesabiwa haki kwa imani, tunahitaji kukua katika mwenendo na mahusiano ya haki. Tunahitaji kukua ili kukumbatia injili na kuwasilisha kwa wengine Mungu. Hebu tumtazame Yesu pekee!

Barua ya Warumi ni hazina ya imani ya Kikristo, imepangwa vizuri na inafahamika kuliko barua zake zote. Ni barua ya kawaida inayokamilisha mpango wa msingi wa kazi za kichungaji. Inazungumzia Neema kwa kuongozwa na Roho wa Mungu. Barua hii imebadilisha mioyo ya wengi waliyoisoma. Neema ndiyo mojawapo ya tofauti kubwa kati ya Ukristo na dini nyingine. Paulo aliandika barua kwa Warumi kuwajulisha kuhusu injili, kwamba haki Yetu yatoka kwa Yesu tu na kwamba hatuifanyii kazi. Tunaokolewa kwa matendo, Matendo ya Yesu msalabani. Hatuokolewi kwa matendo yetu sisi binadamu.

Barua hii ni kitabu kingine cha injili! Yaani habari njema za wokovu. Yesu alikufa msalabani kwa ajili yetu. Basi imani inakuja kwa kusikia, na kusikia huja kwa Neno la Mungu. Wana miguu mizuri wapelekao injili ili wengine wasikie. Paulo anakumbusha mwanamke kuoa mwanamke, au mwanaume kuoa mwanaume yaani ushoga ni dhambi, na kinyume cha asili ya matumizi; na kuna malipo ya upotevu huu. Paulo anatukumbusha jinsi dhambi ilivyo mbaya kwa sisi binadamu na hata viumbe vyote, maana viumbe vyote vinaugua na kupata adhabu kwa ajili ya dhambi yetu sisi binadamu. Baada ya uumbaji wanyama hawakula wanyama wengine, na wala maumivu, huzuni na vifo havikuwepo. Bali baada ya ile dhambi ya binadamu, viumbe vyote vimepata adhabu, japo havikufanya kosa lolote.

Paulo anatukumbusha sisi wote ni wenye dhambi, na mshahara wa dhambi ni mauti na namna tunavyoweza kuhesabiwa haki na Mungu Mwenye haki. Anauliza mwenye dhambi awezaje kuishi siku kwa siku kwa utukufu wa Mungu? Paulo aliona yale mabaya ambayo hataki kutenda, ndiyo anayoyatenda na yale mazuri ambayo anataka kutenda hayatendi, akaugua akisema "ole wangu mimi masikini, ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? Anamshukuru Mungu atupaye ushindi wa dhambi. Asema uovu waja kwa watu wasiomkubali Mungu kama Mwumbaji wa yote, wakifikiri wanajua kila kitu, na wanakataa kufuata njia Yake. Ni vigumu Mungu kuwasaidia watu kama hawa, na jinsi muda unavyoenda wanajifunga katika mafundisho yao ya uongo.

Kwa ujasiri Paulo anaandika "Kwa maana siionei haya injili; kwa maana ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na hata kwa mtu wa taifa jingine pia." Mtu wa mataifa ni kama wewe na mimi. Haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, kutokana na imani, kama Mungu alivyosema, "mwenye haki ataishi kwa Imani." Hii ina maana ya kuwa hatuhesabiwi haki kwa

matendo ya sheria, bali kwa neema ya Mungu, kupitia imani kwa Mwana Wake Yesu aliyetufia tulipokuwa wenye dhambi na si wakati tukiwa wema. Anauliza "ni kitu gani kitatutenganisha na upendo wa Yesu? Je ni njaa, shida, dhiki, au mauti?" Akagundua kuwa mauti, malaika, uzima, hata mamlaka hayawezi kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu BWANA wetu.

Wayahudi walifikiri kutahiriwa au kuwa wana wa Ibrahimu ndiyo kutawaokoa. Anasema tohara ya kweli ni mabadiliko ya kweli ya moyoni; yaani kumpenda Mungu kwa kupokea Kafara ile ya Kalvari, na wala si matendo ya mwili kama ya kutahariwa. Anatoa mfano wa Ibrahimu alihesabiwa haki na Mungu hata kabla ya tohara. Hakuna kitu tunaweza kufanya ili kupata wokovu, au kujiokoa, hata iwe ni matendo mazuri. Kuwa Myahudi, dini fulani, au rangi fulani hayo yote ni bure tu. Ni rehema ya Mungu na neema Yake tu yaweza kutuokoa. Mungu ameonyesha neema na Rehema Yake kwa kumtuma Mwana Wake Yesu Kristo afe msalabani, kwa ajili yetu.

Hii ni kwa kuwa "wote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, na kwamba mshahara wa dhambi ni mauti." Paulo anaendelea kusema kuwa, "nia ya mwili ni uadui wa sheria", ila tukimkabidhi Yesu maisha yetu atatuwezesha yote. Maana hapo tutakuwa hatutawaliwi na dhambi bali na Roho wa Mungu. Tukimkiri Yesu ni BWANA na Mwokozi, kwa midomo yetu na kuamini kwamba amefufuliwa toka kwa wafu, hapo tunaokolewa na kuzaliwa upya. Yatupasa tuishi maisha yetu kwa kumtukuza Mungu. Twapasa tutoe miili yetu kuwa dhabihu hai, tukimwabudu Yeye aliyetuokoa kwa kusulubishwa msalabani kwa ajili yetu. Hebu na tusione aibu kuwaambia watu kisa cha Upendo wa Mungu kwa unyenyekevu na upendo ili wote "wasipotee bali wawe na uzima wa milele."

Tunapatanishwa na Mungu kikamilifu kwa Kifo cha Mwana Wake Yesu msalabani. Dhambi ilikuja kupitia mtu mmoja Adamu, na kuondolewa kupitia kifo cha Yesu kama zawadi yetu wote binadamu. Tunazaliwa mara ya pili, kwa kumkiri Yesu Mwokozi, na kubatizwa. Dhambi zetu zinasulubiwa na hatuko utumwani tena bali tunakuwa huru. Ni Muhimu tumkiri kwa midomo yetu kwamba ni BWANA. Japo Waisraeli kwa pamoja walimkataa Kristo kuna wengi Wayahudi wataokolewa kwa imani. Kwa ajili ya dhambi zetu, Mungu alijitenga nasi, ila alimtuma Mwanawe wa pekee, Ambaye aliishi maisha ya ukamilifu, na Yesu akafa kwa ajili yetu, ili atuondolee dhambi zetu. Yatupasa tumsadiki na kumwamini Mungu, Naye atatutunza na kutuongoza katika yote. Mungu ametufanya sisi tuwe tofauti na wengine na anatupenda upendo wa milele.

Paulo anashauri tutii mamlaka ya serikali zilizowekwa; maana mamlaka ni watumishi wa Mungu, wanaowahudumia watu. Mamlaka zimewekwa na Mungu, na kawaida mamlaka haitoi adhabu kwa wale watu wanaoishika sheria. Tuipende na kuiombea Serikali yetu. Tusiwiwe na watu chochote isipokuwa upendo. Wokovu wetu u karibu kuliko tulivyoanza kuamini. Chochote tufanyacho tufanye kwa moyo, kama vile tunamfanyia Mungu Mwenyewe. Anasisitiza waumini wote wapendane. Paulo anasisitiza tuepukane na mafundisho ya uongo ambayo hayapatani na Biblia. Tutoe miili yetu kuwa dhabihu iliyo hai, ndiyo impendezayo Mungu, maana mambo

ya kutoa kafara ya kuchinja kondoo yamepitwa na wakati kwa sasa baada ya Yesu kufa. Tusijitape na mambo makuu bali tuwe na unyenyekevu, na manyonge.

Tusilipe ovu kwa ovu, tumwachie Mungu kulipiza kisasi. Adui yetu akiwa na njaa tumpe chakula, akiwa na kiu tumpe maji. Tushinde ubaya kwa wema. Tusidaiwe chochote isipokuwa upendo, maana tukipenda tumeitimiza sheria. Tumpende Mungu na wanadamu. Hatuwezi kugusa mbingu bila kugusa wanadamu. Usiku umeendelea sana mchana umekaribia, Yesu karibu anarudi. Wokovu wetu u karibu kuliko jana. Tuyavue matendo ya giza na kuvaa silaha za nuru, tukienenda kwa adabu. Tumvae Kristo tu. Kwa kifupi, Kitabu cha Warumi chaeleza Mpango wa Mungu au ramani ya wokovu, wazungu wanaita GPS (God's plan for Salvation). Naweza kusema kwamba sura ya 5 ndiyo kiini chake! Yaani wakati bado tupo dhambini Mungu alionyesha upendo wake kwetu. " Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. 7 Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema.8 Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.9 Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye.10 Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake." Wayahudi na wote wa nchi zingine tunahitaji wokovu. Na Mungu ametoa wokovu huo kupitia Mwana Wake, aliyekufa msalabani kwa ajili yetu. Zawadi hii inapokelewa kwa imani tu. Ibrahimu aliikubali kwa imani; akapokea wokovu, nayo ni mwanzo tu wa safari yetu na Yesu, na baada ya hapo Mungu huhitaji kuishi ndani ya mioyo yetu kupitia Roho Mtakatifu. Basi watoto wote nasi watu wazima tujue kwamba katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na sote tumpendao katika kutupatia mema. Tu heri binadamu tuliosamehewa makosa yetu, kwa neema ya Mwana wa Mungu.
Paulo anamaliza barua kwa kusalimu marafiki zake wengi, anawashukuru, na kumsifu Mungu akisema "Mungu Ndiye Pekee Mwenye hekima yote. Utukufu una Yeye kwa Yesu Kristo milele na milele, Amina."

*Maombi yenye dhati na yenye bidii ya Yesu yanatofautiana na maombi yetu dhaifu—Kuhusu Kristo inasemwa: "Na akiwa katika uchungu mkubwa aliomba kwa bidii zaidi." Je ni tofauti iliyoje tukilinganisha maombezi haya ya Mkuu wa mbinguni na maombi yetu dhaifu, yasiyojumuisha moyo, ambayo hutolewa kwa MUNGU. Wengi wanaridhika na huduma ya mdomo, na ni wachache walio na shauku ya dhati, ya bidii, na ya upendo kwa MUNGU.

----------------------------

Maswali: Paulo aliandika kitabu cha Warumi akiwa wapi? Paulo anasema tunaokolewa kupitia nini? Kwa nini tutii serikali? Paulo alisema wangapi wamefanya dhambi? Neema maana yake ni nini? Rehema maana yake ni nini? Kwa nini barua kwa Warumi ni kitabu cha injili? Kwa namna gani viumbe vyote vina huzuni kwa ajili ya dhambi zetu binadamu? Je, Kwa nini mazuri tunayotaka kuyafanya hatuyafanyi bali mabaya tusiyotaka kuyafanya, tunajikuta tumeyafanya? Upendo unatimizaje sheria? Kwanini afya na wokovu vinafanana sana? Kwasababu wenyewe hatujiwezi, kwanini ni muhimu basi kuomba kabla ya kusoma Biblia?

**SIKU YA 329**
**(Novemba 24)**

**Wakorintho wa kwanza.**

# Shida za waumini wapya zajadiliwa.



Barua hii ndefu inayozungumzia mambo ya kiroho, iliandikwa Kiyunani kwenda kwa waumini wa Korintho huko Uyunani pengine katika mwaka wa 55 BK. Paulo alipanda hili kanisa, alipohubiri na kuishi mwaka na nusu mahali hapa. Jiji la Korintho ya kale lilikuwa la kimataifa. Uhamiaji, shuguli zenye kuleta pesa, matukio makubwa ya michezo, karamu kubwa, tamaa mbaya za mwili kama uasherati, uzinzi na mmomonyoko wa maadili ni baadhi ya matukio yaliyoendelea huko. Anaandika kwa viongozi na washiriki akishughulikia shida za waumini. Shida hizi tunazo hata leo kwenye makanisa yetu. Kwanza ni malumbano ya washiriki, kwenye hili kanisa. Walikuwa wanagombana wenyewe kwa wenyewe. Paulo anasema Wayahudi wanatafuta ishara na Wayunani hekima bali wao wamtafute Yesu aliyesulubiwa. Wengine walisema wao ni wa Paulo na wengine ni wa Apolo na Kefa, akauliza "Je Kristo amegawanyika? Je Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu? "Je mlibatizwa kwa Jina la Paulo au la Yesu?

Paulo anasema wao ni watenda kazi tu katika shamba la Mungu au watumishi wa Kristo. Anasema wamepigwa, wamepatwa na njaa, wameaibika, na kuwa takataka za dunia ili Kristo atukuzwe na wala si wao. Tujihadhari kugombana gombana kama watu wa dunia. Hata leo inabidi tuepuke mambo ya malumbano na wenzetu. Tutafute ufumbuzi, tuwekane sawa na tujue kutunza amani tunapocheza, au kufanya kazi na wenzetu. Kisha Paulo anazungumza uovu uliokuwa unaendelea kanisani, wa uzinzi, maana kuna mtu alimchukua mke wa baba yake kuwa mke wake. Huu ni uovu wenye aibu na kuleta masikitiko, na aliwaambia apaswa atengwe na kupewa karipio na adhabu ili aweze kusaidiwa na kuokolewa.

Akashauri wasijichanganye na watu wazinzi, wenye kutamani au wanyanganyi, au wadhalimu maana hao hawatairithi mbingu. Akawakumbusha kwamba "miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu, sisi si mali yetu wenyewe." Hivyo tunapokula au kunywa au kufanya lolote, tukumbuke tusifanye uovu kwenye miili yetu maana hatujajiumba, bali tulinunuliwa kwa thamani kubwa ya damu ya Yesu. Hivyo tumtukuze Mungu katika miili yetu. Hatuwezi kusema tunaweza kula chochote hata cha kutudhuru kama sigara, chakula kibaya au pombe. Hatuwezi kujifanyia lolote tupendalo na kusema "mwili ni wangu" maana sisi tumeumbwa na Mungu. Sisi ni mawakili tuliopewa jukumu na tutawajibika hukumuni.

Anasema siku zile watu wengine walikula vyakula ambavyo vimetolewa kwa miungu na sanamu, na hiyo ni dhambi. Paulo anasema muhimu kwake, ni kutojua mengi ya hapa duniani, ila Yesu Kristo aliyesulubishwa. Paulo anazungumzia Meza ya BWANA au Pasaka kwa undani akisema kabla ya mtu kupokea Sakramenti hii, ni lazima ajihoji, kama ana uovu wowote kisha aungame. Mkate unawakilisha mwili wa Yesu na divai inawakilisha damu ya Yesu na tukiwa tunashirki "tunakitangaza kifo Chake hata ajapo." Ni sakramenti ya utakaso pia. Paulo anatoa ushauri wake binafsi, na kusema ni vyema mtu asioe, ila kama hawezi kuishi mwenyewe basi aoe. Ni dhambi kuishi na mtu bila kuwa na ndoa takatifu iliyofungwa kisheria. Ndoa inaweza kuwa ya jadi, ya kanisani au ya serikali, ila ukiweza kufanyia kwenye kanisa itakuwa bora zaidi kwani utaombewa ndoa yako pia! Ameona kwamba kutooa mara zingine kunasaidia kufanya kazi ya Mungu kwa mvuto mkubwa. Ila yeye aliyeoa tayari anaposoma ujumbe huu tayari asimwache mke wake; pia yule aliyeoa mtu asiyemwamini Mungu, asimwache. Maana huyo akiongoka aweza kumsaidia kupata wokovu kama atakuwa akiishi pamoja naye. Ila wanaomjua Mungu wao wasifungiwe nira au ndoa na watu wasioamini. Mume na mke waishi kwa upendo na unyenyekevu. Watu wote waepuke uchafu wa kuishi na mwanamume au mwanamke bila mipango ambayo Mungu ameagiza. Ndoa iwe na usafi na heshima.

Paulo alisikia waumini wanapelekana mahakamani kushitakiana. Akauliza "Je hamwezi kuyatatua hayo mambo kanisani? Hamjui kwamba watakatifu watahukumu ulimwengu?" Kama tutahukumu ulimwengu wote hata malaika waovu, kwa nini basi tushindwe na kesi hizi ndogo ndogo ndicho alichosisitiza? Mtume anawaambia watu kuhusu karama au zawadi za roho "kila mtu amepewa karama za Roho, ili kumnufaisha mwingine." Pengine ni uwezo wa kufundisha mwingine, kuimba, maneno ya hekima, au maneno ya maarifa, kumsaidia mtu apone, na wengine matendo ya miujiza, unabii, kupambanua roho au uwezo wa kunena lugha tofauti. Roho wa Mungu hugawa hizo karama kwa kila mtu. Wengine karama moja wengine zaidi, kwa jinsi Mungu apendwavyo.

Hivyo tusione wivu mwenzetu akiwa na kipaji au karama fulani, maana Mungu anajua kile cha kutufaa, na hata hivyo tuna karama fulani ambayo mwingine hana. Anazungumza kuhusu upendo baada ya kuzungumzia karama kwamba kila karama itumiwe kwa upendo la sivyo itakuwa sifuri katika kazi ya Mungu. Hakika upendo ndiyo karama kuu, ndiyo siri niliyojifunza hapa. Je, tunawezaje basi kuwa na upendo usio feki? Vizuri leo upange kukariri sura hii ya 13, inayohusu upendo. Ni muhimu tujue upendo ni nini. Upendo ni zaidi ya hisia, au mihemko, au mahaba,

ni kanuni ya mbinguni. Mungu ni upendo, Yesu alikuja kudhihirisha upendo wa Mungu. Upendo ndiyo Amri kuu kwenye Sheria. Kumpenda Mungu kwanza kwa mioyo yetu yote, nguvu, roho na akili zetu zote, na kumpenda jirani kama nafsi. Anatuambia tukisema kwa lugha za Malaika na hatuna upendo ni bure kabisa, na hata tukiwa na imani ya kuhamisha milima, na kujua siri za unabii kama hatupendi watu na Mungu tunajisumbua na kujichosha mno.

Asema upendo wa Kweli "huvumilia, hufadhili, hauna chuki, hautabakari, haujivuni, haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, hauoni uchungu, hauhesabu mambo mabaya, haufurahii udhalimu. Upendo huvumilia yote, huamini yote, hutumaini yote, hustahimili yote. Basi mambo ya kudumu ni imani tumanini na upendo na kilicho kikubwa katika hayo ni upendo. Upendo ndiyo sababu ya Yesu kufa kwa ajili yetu. Upendo huu ni wa vitendo, si porojo za maneno tu! Je, unajua tofauti kati ya mtu mwenye upendo wa Kweli, na yule mtu wa upendo wa maneno? Upendo kwa vitendo ndiyo changamoto yetu. Paulo anasema vilivyobakia duniani ni imani, tumaini na upendo, na kubwa kupita vyote ni upendo, yaani upendo wa Kweli.

Paulo anazungumzia kuhusu ufufuo siku ya mwisho kwamba kufumba na kufumbua tutabadilishwa miili yetu ivae kutokufa, yaani isiwe ya kufa tena. Malaika watapiga tarumbeta ya mwisho, wafu watafufuliwa toka makaburini mwao, na mwili wa kuharibika utavikwa kutokuharibika, na mwili wa kufa utabadilishwa usife. Mauti itamezwa na kushindwa, ndipo wote tutafurahi, na kusema "u wapi ewe mauti uchungu wako?" Hebu tupate faraja tukisoma fungu hili kwani wengi tumepoteza wapendwa wetu. Tumelia kwa huzuni, ila mtume huyu anatupa faraja na kutueleza kwa kina, kifo ni nini na nini kitatokea kwa wafu waliokufa katika BWANA.

Paulo anazungumza kwenye Sura ya 16 anazungumza kuhusu ukusanyaji wa sadaka ili akija kuwatembelea, waweze kuziwasilisha pale penye mahitaji ya injili. Je, kutoa sadaka kuna faida gani leo kwetu? Kumshukuru Yesu kwa dhabihu aliyotoa kwetu na baraka Zake, huonyesha kujisalimisha kwetu kwa Mungu, huonyesha kwamba tunamwamini, na kudhihirisha upendo wetu kwa Mungu na jirani yetu, itatusaidia tukopeshe ila hatutakuwa na madeni tunapofuata kanuni Zake. Kutoa kunatusaidia kukataa kupenda pesa n.k. Tumeambiwa madirisha ya mbinguni ya baraka yatafunguliwa kwaajili yetu na siyo milango tunapofuata maagizo ya Mungu ya utoaji (Malaki 3). Umejiuliza kwanini? Mimi nilihesabu madirisha ya nyumba nayoishi nikayakuta yako 28, na milango mitatu, pengine hii ina maana kwamba baraka zikipitia madirishani zitakuwa nyingi kuliko zikipitia milangoni!

Maisha ni magumu kwa kila mtu anayezaliwa kwenye ulimwengu huu wa dhambi. Kila mtu ana matatizo yake. Faida kubwa waliyo nayo Wakristo ni kwamba Kristo Yuko kando yao ili kuwasaidia kubeba au kutatua matatizo yao. Hivyo amani waliyo nayo Wakristo haitokani na kukosekana kwa changamoto, bali ule Ukweli kwamba Mungu Yuko pamoja nao katika majaribu yao. Paulo alilemewa kupita kiasi, yaani kupita nguvu zake, hivi kwamba alikata tamaa hata ya kuishi! Mateso yake yalimfanya aone hitaji la kumtegemea Mungu pekee, na Mungu akamsaidia. Kama vile Paulo alivyofanya, Wakristo tunapaswa kuwapa wengine faraja kutoka kwa Mungu. Kwa kufanya hivi, tunawaelekeza kwa Mungu ambaye peke yake

Ndiye anayeweza kumsaidia mwanadamu kufikiri katika ulimwengu huu wa mateso. Ni nani anayeweza kufanya lolote bila Mungu? Hakuna mtu! Tusisahau kwamba "mwenye kuvumilia hata mwisho ndiye atakayeokoka." Mathayo 24:13. Kwa hiyo, tuombe neema kila siku ili tuishi siku moja baada ya nyingine kwa ahadi ya Mungu kwetu ni, "Neema Yangu yakutosha; maana uweza Wangu hukamilishwa katika udhaifu." 2 Wakorintho 12:9 !

*Fuata Kielelezo cha Yesu kwa Kuanza Siku kwa Sala—Ilikuwa katika saa za sala ya peke yake ndipo Yesu katika maisha Yake duniani alipata hekima na nguvu. Hebu vijana wafuate mfano Wake katika kutafuta alfajiri na jua lizamapo magharibi, muda wa utulivu kwaajili ya ushirika na Baba yao aliye mbinguni. Na pia wainue mioyo yao kwa MUNGU siku nzima. Katika kila hatua ya njia zetu anasema, 'Kwa maana Mimi, Bwana, MUNGU wako, nitakushika mkono wako wa kuume, Usiogope; nitakusaidia.. Isaya 41:13. Laiti watoto wetu wangeweza kujifunza masomo haya katika miaka yao ya awali, ni upya na nguvu, furaha na utamu wa jinsi gani, ambao ungeletwa maishani mwao!
---------------------------

Maswali: Kwa nini ni vibaya mtu kuoa ndugu wa karibu? Kwa nini ni vibaya waumini kupelekana mahakamani? Kwa nini hatuwezi kujiokoa kwa matendo yetu? Ni nini maana ya 'mwili wetu ni hekalu la Roho Mtakatifu?' Kariri Wakorintho 13:4-8 upendo wa Kweli una tabia gani? Sakramenti ya Meza ya BWANA inasimamia nini? Kwa nini "Tukijua kuzungumza lugha zote ni 0, tukijua kuzungumza lugha kama malaika ni 0, tukijua unabii wote ni 0, tukijua siri za mbinguni ni 0, tukiwa na imani ya kuhamisha milima ni 0." Kwa nini Wakorintho waambiwa Kristo hakugawanyika? Kwa nini muumini awe makini kabla ya kuamua kumpeleka mwenzake mahakamani? Je, wale watu wanaoiba pesa za kanisa washitakiwe mahakamani au waachiwe tu? Wafu watatoka kaburini kwa namna gani? Je, ungependa Mungu afungue madirisha ya mbinguni kwako kwa namna gani mwezi huu?

**SIKU YA 330**
**(Novemba 25)**

**Wakorintho wa pili.**

# Tunapokuwa wanyonge ndiyo tuna nguvu.



Mtume Paulo aliandika barua hii kwa Wakorintho wa Uyunani (Ugiriki) akitetea utume wake, na injili. Maandishi yake yanaonyesha alikuwa na barua kama nne hivi Kwa Korintho, ila mbili ndizo tulizonazo leo. Paulo alipewa utume na Yesu Mwenyewe. Anasema yeye siyo duni kati ya mitume walio wakuu kwa lolote ijapokuwa pia yeye si kitu. Anawaandikia barua ya karipio kama baba yao ili atakapokuja "asiutumie ukali kwa kadri ya uwezo ule aliopewa na BWANA, kwa kujenga wala si kwa kubomoa." Paulo aliahirisha safari yake Korintho, ili apunguze masikitiko, kwani wengine hawakumwelewa na wakamfanya alie machozi. Alitaka kuwavuta watu kwa Kristo, bali wengine walitaka kuficha uovu na kuligawanya kanisa.

Paulo anawapongeza Wakorintho baada ya kumshughulikia yule aliyekosa kwa kuishi na mama yake wa kambo, na anawasihi wamsamehe na kumrudisha kwenye ushirika tena ili Shetani asiwashinde kwa dhambi ya kutosamehe na kukosa upendo kwa yule aliyejirudi; na mkosaji akamezwa na huzuni ipitayo kiasi. Kila mara

tunakutana na manabii wa uongo, watu wanaojiita manabii au mitume, walio na injili yao wenyewe, siku hizo walikuwepo pia hao, wale waliosema wao ni wafuasi wa Musa na Yesu ila walifundisha kwamba sheria za Wayahudi za kutoa kafara na zinginezo zilikuwa zinaendelea. Manabii wa uongo hata siku hizi wanajitukuza wenyewe na kusema kuhusu huduma zao, na kutafuta sadaka zaidi ya kondoo wa Mungu. Na sisi leo tunashauriwa kujiepusha na manabii hao wa uongo, na kuwa harufu ya manukato ya Kristo mbele za Mungu. Mtu mmoja alisema, Yesu alilisha watu 5000, ila manabii wa uongo wanatafuta washiriki 5000 walishe matumbo yao, wanatembea na magari mazuri kupita kiasi, na hata ndege.

Paulo anasema wale wote wanaomfuata na kumtumikia Mungu wakati mmoja au mwingine watapitia mateso, ila Mungu ana faraja kwa kila mmoja wetu. Mungu amekuwa faraja kwa wale wote wenye shida, na hasa wale wanaompokea na kutafuta kufanya Mapenzi Yake. Katika matatizo na shida zote tukumbuke kwamba Mungu Ndiye Mweza na yote yanawezekana Kwake. Mungu aweza pia kutumia waumini wengine kuwa faraja kwa wale wanaopitia shida. Twaweza kuwaombea marafiki, au ndugu zetu wanaopitia shida. Dhuluma au shida za Yusufu Misri zilimfanya aimarike na kutakasika. Japo mtume Paulo na wenzake waliudhiwa, na kupata dhki nyingi, waliona dhiki zao ni nyepesi na za kitambo ukilinganisha na ule uzuri wa Kristo. Anatushauri tuviangalie vile visivyonekana vya milele, na si vya sasa vinavyong'aa na vya kitambo tu. Anatupa wosia kuenenda kwa imani, na si kwa kuona. Hata watu wakiwaona wao ni wenda wazimu waliorukwa na akili, ni kwa ajili ya kukazana kuhubiri injili, maana upendo unawabidisha. Hawataki watu waangamie.

Yesu ametupatanisha Na Mungu, kwa kifo Chake. Hiyo ndiyo sababu tosha ya kutufanya tusijifikirie wenyewe tu, bali Yeye aliyekufa kwa ajili yetu. Twapasa tuishi maisha ya utakatifu yasiyo na lawama wala madoa au makunyanzi. Kwa kuwa Mungu ni Mtakatifu, nasi twapaswa tutafute utakatifu na amani na watu. Paulo anawaambia washiriki waweke sadaka maalumu, kwa masikini na wenye mahitaji, maana Mungu ana thawabu yao. Anawapongeza washiriki wa Makedonia waliokuwa na ukarimu wakisaidia kazi ya Mungu, wakijua kwamba Mungu atawasaidia katika kila hitaji lao. Hebu tutoe kutokana na tunavyobarikiwa, si mali tu maana Mungu ana kila kitu bali pia mioyo yetu, burudani zetu na muda. Ni sisi ndiyo ametupa uchaguzi wa kumtolea nini, na kiasi gani. Apandaye haba huvuna haba. Tusijaze vichwa na Maandiko, na kuacha mioyo yetu iwe michafu kwa dhambi.

Paulo anasisitiza Wakristo wawe wanyenyekevu, akijua wengi wamepotoka kwa kufikiri unyenyekevu ni unyonge. Unyenyekevu ni kuwa na nia ya Yesu. Paulo anasema ndoa ni taasisi ambayo Mungu aliiweka, na kwamba mtu asifunge ndoa na mtu asiyeamini. Niambie rafiki yako ni nani nami nitakuambia wewe ni mtu wa namna gani! Ndege wanaofanana huruka pamoja, wengi pia wamechukua mtandao kuwa rafiki, na hili lifanye tujiulize kwamba tunatumia muda gani, na ni nini tunaangalia humo. Je, tunawaambia watu habari njema kwenye mtandao pia, yaani umishenari wa kidigitali. Mtu asiyeamini anathamini mambo tofauti na yule anayeamini. Jinsi ambavyo maji na mafuta visivyoweza kuchangamana, na ndivyo ambavyo ufalme wa Mungu usivyochanganyika na ufalme wa adui. Anasema "injili

imesitirika kwa wanaopotea, ambao ndani yao Mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao." Paulo anakazia dhiki na shida zetu ni ndogo, na za kitambo kidogo tu, ukilinganisa na ufalme wa mbinguni wa milele. Mtu mmoja amesema "tutakapofika mbinguni, tutajaribu kukumbuka kwa bidii kuhusu huzuni na shida zetu za dunia, ila zitapelea sana ukilinganisha na uzuri wa mbinguni, na kule kuishi na Mungu, uso kwa uso", Je, hii si habari njema ya kutuletea tabasamu kama wasafari na wahujaji wa dunia hii?

Hivyo basi, tusiviangalie vinavyoonekana bali visivyoonekana, kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu, bali visivyoonekana ni vya milele. Leo ndiyo wakati uliokubalika kwetu na siku ya wokovu wetu. Yesu alikuja na kuishi maisha ya umasikini, japo alikuwa tajiri, ili nasi tupate kuwa matajiri kwa umasikini wake. Paulo anasema amepata shida nyingi na masumbufu, kwa kupigwa bakora, kupigwa mawe, kuvunjikiwa jahazi, kusafiri kwenye mito ya hatari, kuingiliwa na majambazi, hatari za taifa Lake Israeli, njaa, kiu, kufunga, baridi, kutokuwa na nguo na mengi wakati akililiangalia kanisa. Anasema hana budi kujisifu kwa dhiki hizi, japokuwa haipendezi! Ila Anajifisia udhaifu wake, maana anapokuwa dhaifu, ndiyo ana nguvu katika Kristo.

Analeta fungu ambalo twaweza kuomba kuondoa mawazo mabaya na kuangusha ngome za adui. "Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu na tukiiteka nyara kila fikra ipate kumtii Kristo." Elezea siri hii kwa watoto waijue vizuri! Kwa makusudi asipate kujivuna kupita kiasi. Kwa wingi wa mafunuo Mungu alimpa mwiba kwenye mwili wake. Mjumbe wa Shetani alimpiga asije akajivuna. Naye Paulo alimsihi BWANA mara tatu kwamba kitu kile kinachomletea maumivu na udhaifu wa afya kimtoke, ila hakikumtoka. Mungu alimwambia "Neema Yangu yakutosha, maana uweza wangu hutimilika kwa udhaifu." Paulo akasema atajisifia kwa udhaifu, na kuwa na furaha nyingi, ili uweza wa Kristo uwe ndani yake. Anasema anapendezwa na udhaifu, shida, dhiki na huzuni, maana anapokuwa dhaifu ndiyo anapokuwa na nguvu za kiroho na za kumshinda mwovu.

Paulo alikuwa mchapakazi. Hakuwalemea washiriki wake kwa kuomba pesa, bali alitengeneza mahema. Kwa kujitegemea alikidhi mahitaji yake na ya wengine pia. Kwa sababu kanisa ndiyo lilikuwa linaanza, Paulo anatumia muda kuwaeleza uzoefu na aliyopitia kwenye huduma, maana wengi walikuwa wakisema maneno ya kudharau huduma yake. Hapendi kujisifu na anakazia wote tunapotaka kujisifu, tujisifu kwa kumjua BWANA.

Basi sote tujifunze toka kwa Paulo kwamba tukiwa katika Kristo tumekuwa viumbe vipya, ya kale yamepita na tazama! Tumeanza maisha mapya ya kuwa watoto wa nuru. Ahadi moja nzito kwenye kitabu hiki ni ile sura ya kwanza 1:20 "Kwa maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika Yeye ni Ndiyo; tena kwa hiyo katika Yeye ni Amin; Mungu apate kutukuzwa kwa sisi." Hakika Biblia ni bustani ya Mungu ya thamani, na ahadi Zake ni vito vya ajabu. Maandiko yote yanapaswa kupokelewa kama Neno la Mungu kwetu, yaani kama anazungumza nasi ana kwa ana. Hebu sote tuweze kuziamini ahadi za Mungu. Hatupaswi kuangalia ndani ya mioyo yetu

kama tuna hisia za furaha kama ushahidi wa kukubalika kwetu na Bwana, lakini tunapaswa kuchukua ahadi za Mungu na kusema “ahadi hizi ni zangu. Amini kwamba umepokea kile unachoomba, na utakuwa nacho.’ Kwa imani tumshike Kristo, Naye atatuwezesha Tumshukuru Mungu kwa kuwa tuna Mwokozi.


*Ikiwa Yesu Alihitaji Kuomba Akiwa Duniani, sisi tunapaswa kusali zaidi kwa kiasi gani basi—Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, Aliwafundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba. Aliwaelekeza kuwasilisha mahitaji yao ya kila siku mbele za MUNGU, na kumtupia/kuitwika mizigo yao yote Kwake. Na uhakikisho aliowapa kwamba maombi yao yatasikilizwa, ni uhakikisho kwetu pia.
-----------------------------

Maswali: Kwa nini Mungu hakutoa ‘mwiba wa Paulo?’ Kwa nini mtu anayemwamini Mungu asioe mtu asiyemwamini Mungu? Kwa nini ni muhimu waumini kutoa sadaka? Kwa nini tusiviangalie vitu vinavyoonekana?

**SIKU YA 331.**
**(Novemba 26)**

**Wagalatia.**

# Tunda la Roho dhidi ya matendo ya mwili.



Wagalatia ni sehemu ya Uturuki leo. Paulo alitembea huko katika safari zake za kuwaambia watu kuhusu Yesu, kwa mara ya kwanza katika makanisa ya Apisidia, Antiokia, Ikonia, Lystra, na Derbe. Mtoto wake katika imani Timotheo alitoka Derbe. Paulo aliandika Barua hii kuwaambia Wagalatia kwamba utume wake ni BWANA alimpa na si mwanadamu. Mkazo wake ulikuwa wokovu hautokani na matendo ya binadamu, maana Wagalatia wengi walifikiri kutahiriwa na kuwa Myahudi ndiko kutawafikisha mbinguni. Aliwaambia wanaoshurutisha watu kutahiriwa au kufuata matendo ya sheria wao wenyewe hawaishiki sheria, bali wamekazania kutahiriwa kwa mwili. Anawaambia Wagalatia hawatumii ubongo wao vizuri, kwani ni nani ataokolewa kwa matendo yake mazuri au kutahiriwa? Hakuna hata mmoja! Kila binadamu ameoza na uovu. Uwe uovu mdogo au mkubwa.

Ni tendo la Yesu tu msalabani linatuokoa. Anasema kwamba kama kuna mtu anayewahubiri mambo ya uongo huko Galatia, mbali na yale ya injili aliyowafundisha basi na alaaniwe. Anawakumbushia kuwa walianza vizuri katika mambo ya kiroho bali wakakwazika kuingia katika matendo ya mwili. Anawapa changamoto Wagalatia kwamba kama wanafikiri kukata kipande kidogo cha miili yao kitawapa wokovu, basi wakate kipande chote. Mtume Petro naye alikwazika na kuingia kwenye hili, baada ya kukaa Galatia kwa muda, akiwa na waumini wa Kiyahudi au 'watu wa tohara' kama walivyojulikana akanza kuona aibu kula na watu wa mataifa waliokuwa Wakristo, akitaka kuwafurahisha Wayahudi, na kufikiria zaidi yale wanayomfikiria.

Paulo akampa onyo na Petro akaona kosa lake, kwamba kuweka mawazo ya watu wengine badala ya mwongozo wa Mungu ni kupotosha Neno la Mungu wanapowahubiria mataifa; maana ni Yesu tu atakayewaokoa. Matendo fulani kama

vile kuchanja mwili, kwenda kuhiji mahali au hata matendo yahusikanayo na dini hayatatuokoa. Mungu Ndiye wokovu wetu, huyu tumtafute na kumkubali kwanza, ndipo yale matendo yanakuwa tunda la imani yetu. Mungu hatofautishi watu wa mataifa na Wayahudi, wanawake au wanaume, watu huru au watumwa, matajiri au masikini, warefu au wafupi, weusi au weupe.

Paulo aliona wengine wanachezea neema ya Mungu, jambo ambalo linatokea hata leo. Wengi husema hawajali wakiwa wanavunja sheria kwani wameokolewa na neema. Ni kweli wote tunaokolewa kwa imani peke yake, imani yetu kwa Mungu na Mwana Wake na siyo matendo yetu. Ila kuokolewa kwa neema haina maana sasa tufanye matendo maovu. Lazima tusulubiwe au kujisalimisha kwa Mwana wa Mungu na kufa au kuyaacha matendo maovu na kushikilia matendo mapya. Paulo anasema "Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi Yesu aliyewaita katika neema na kugeukia injili ya namna nyingine, basi yoyote anayehubiri tofauti na injili alaaniwe." Hatuhesabiwi haki na Mungu kwa matendo ya sheria, maana kwa matendo ya sheria hakuna binadamu anayaweza kuhesabiwa haki.

Ni kweli tunahitaji kuhesabiwa haki, maana tunaanguka na kukosa mara nyingi. Wale ambao wana imani ni watoto wa Ibrahimu, baba mwenye imani. Maana Wayahudi wengi walijivuna wao ni watoto wa Ibrahimu, na Paulo akawakumbusha kama wao ni wa Kristo basi wamekuwa watoto wa Ibrahimu. Paulo anasema sisi tu watoto wa Sara au watoto wa ahadi, si watoto wa Hajiri, ni watoto ambao tupo huru, tusijiweke utumwani kwa matendo ya sheria. Paulo asema walianza mbio vizuri na sasa wanaharibu kazi njema, kwa kukazania matendo ya mwili, na kutahiriwa. Anawaambia "waenende kwa Roho, wala hawatazitimiza kamwe tamaa au mambo ya mwili"

Wagalatia inatufundisha tunda la Roho ambalo kila mtoto wa Mungu anapaswa awe nalo ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi. Hebu kariri tabia hizi zote. Kinyume cha tunda la Roho ni tunda la mwili au tamaa za mwili. Nazo ni kujisifu, kuchokozana na kuoneana wivu, uchawi, ibada ya sanamu, faraka, uzushi, uasherati, ufisadi, uchafu, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, husuda, ulevi, ulafi na mambo yanayofana na hayo. Watu watendao mambo haya maovu, hawawezi kuurithi ufalme wa Mungu. Daima tuwe na upendo kumrudisha mtu aliyeghafilika kufanya makosa au kutenda dhambi, tumrejeshe upya mtu huyo kwa upole kwa Yesu, ila tuangalie nafsi zetu tusije tukajaribiwa. Tuchukuliane mizigo yetu tukisaidana, kama ndugu na dada maana Baba yetu ni mmoja.

Paulo anatukumbusha kwamba Mungu anajua kila kitu tunachokifanya, cha siri na cha wazi "tusidanganyike Mungu hadhihakiwi. Chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Yeye apandaye matendo ya mwili atavuna uharibifu, ila apandaye matendo ya Roho au ya tunda la Roho basi atavuna hayo. Mtu hawezi kupanda mchicha akavuna bangi. Mungu atusaidie tupige mbio tukisahau yaliyopita. Hebu tuitazame ile zawadi kubwa Yesu ameweka kwa ajili yetu. Kama wanaridha wanavyoshindania vikombe vya ushindi vinavyozeeka, tusishindanie nyumba, baiskeli, magari, utajiri, mashamba, mifugo, nguo nzuri, au vyombo vya kuchezea (toys) bali tupige mbio kupata uzima wa milele katika Yesu.

Hakuna chuo kikuu bora cha kufundishwa kuliko kukaa miguuni pa Yesu, tukingojea hapo kwa utulivu kusikia sauti Yake ikisema nasi kupitia nguvu za Roho Mtakatifu. Shetani anafanya kazi sasa kama alivyokuwa wakati wa Paulo kudanganya na kuharibu roho za watu kwa mafundisho ya madanganyo yake. Kwa hivyo jihadhari na mtu yeyote anayekuja kwako akifundisha kitu kinyume na imani yetu yoyote ya Biblia. Maana yake ni kwamba ni lazima uyajue mafundisho haya ya Biblia vizuri sana, kiasi kwamba mawakala wa Shetani wanapoleta mafundisho yao potofu utagundua makosa na kuyakataa. Ni suala la kufa na kupona, kwa hivyo hili linapaswa kuchukuliwa kwa uzito!

Hebu tuwe na furaha na tukiwa na shida au haja kitu chochote, tumwambie Mungu tusimfiche. Endapo tuna huzuni, hasira au shukurani, tumweleze Mungu na kuzungumza Naye, maana anajali maisha yetu mno.

*Yesu Aliomba Nguvu za kustahimili Majaribu—Wachache watafuata mfano wa Mwokozi wetu kwa maombi ya bidii na ya mara kwa mara kwa MUNGU ili kupata nguvu za kustahimili majaribu, na kuweza kutekeleza majukumu ya kila siku, ya maisha haya. Kristo Ndiye Kapteni wa wokovu wetu, na kwa mateso na dhabihu Yake Mwenyewe, ametoa mfano kwa wafuasi Wake wote, kwamba kukesha kwa maombi na bidii ya kudumu ni vitu muhimu kwa upande wao ikiwa watawakilisha kwa usahihi upendo uliokaa katika kifua Chake kwa ajili ya jamii ya ubinadamu iliyoanguka.

-------------------------

Maswali: Kwa nini hatuokolewi kutokana na kutahiriwa, kabila au dini zetu? Tunda la Roho ni nini? Tunda la mwili ni nini? Kwa nini Paulo alistaajabu kuhusu Wagalatia? Kwa nini inabidi tuondoe hasira, matusi, uchafu, kusengenya, ulevi, na visasi? Je unawezaje kuepuka magomvi? Je, nami nafikiria kupitia haki au matendo yangu naweza kujipatia wokovu? Imba wimbo wa cha kutumaini sina ila damu yake Yesu! Je, unazijua nguzo 28 za imani? Taja 10 kati ya hizo!

**SIKU YA 332.**
**(Novemba 27)**

**Waefeso.**

# Mahusiano ya wazazi, watoto, wake, waume, mabwana na watumwa.



Paulo aliandika barua hii akiwa mfungwa Rumi. Kama tunatala kukariri kitabu kimoja kati ya vile 66 vya Biblia, basi ni hiki! Kwani kitabu hiki kina kila kitu ndani yake, ukilinganisha na vingine, yaani uumbaji, kuja kwa Yesu duniani mara ya kwanza na kufa kwaajili yetu, na kurudi kwake mara ya pili. Yaani toka Mwanzo mpaka Ufunuo! Wakati huu pia Paulo aliandika pia barua kwa Wafilipi, Wakalosai, Filemoni na Timotheo wa pili. Washiriki wa Efeso Uturuki walikuwa watu ambao si Wayahudi. Timotheo alikuwa mchungaji wao, kanisa hili lilikuwa la kwanza kati ya yale makanisa saba aliyoandika Yohana kwenye Ufunuo. Barua hii yaonekana kutoshugulikia shida za washiriki. Efeso ilijulikana kwa hekalu kubwa la mungu wa kike Diana, mungu wa Artemi. Kwenye mji huu wahunzi walimkasirikia Paulo alipokuja kuhubiri kuhusu Yesu maana walifanywa wakose soko la kuuza miungu ya chuma ya Diana. Paulo alimtuma Tikiko aende na barua. Anawasihi Waefeso waishi kwa utume walioitiwa na Mungu. Kitabu hiki kinabubujika furaha katika kumjua Yesu na kuwa na ushirika na waumini wengine. Ni fursa yetu kumjua Mungu na upendo Wake na kuingia katika familia Yake. Tunapaswa kutiwa moyo kwamba kwa neema Yake hakuna kitakachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu.

Kitabu hiki chafanana kiasi fulani na Wakolosai. Paulo anawakumbusha watu kwamba yeye ni mtume na mtumwa wa Kristo na umoja katika mwili wa Kristo ni

muhimu iwe kati ya wazazi, wake, waume, watumwa au watoto. Paulo anatukumbusha "tumfuate Mungu kama watoto wanaopendwa tukatende kwa upendo, kama Kristo Naye anavyotupenda hata akajitoa kwa ajili yetu sadaka na dhabihu kwa Mungu, harufu ya manukato mazuri." Anatushauri tusinene kwa maneno ya kipuuzi wala kuishi maisha ya aibu na uchafu, au kubishana maana hayo hayapendezi. Wosia wake ni "tutende kwa hekima tukiukomboa wakati, kwa maana tunaishi siku ngumu zenye uovu mwingi", tusipoteze muda na hayo.

Anawaambia wake wawatii waume zao, kama kumtii BWANA, kwa kuwa mume ndiye kichwa cha mke wake, kama Kristo alivyo kichwa cha kanisa. Kila mke anapaswa kumweheshimu mume wake, kwamba ndiye kiongozi wa nyumba. Anawaambia wanaume, wawapende wake zao, kama Kristo alivyolipenda kanisa akajitoa na kufa kwa ajili yake. Kuna heshima ambayo tunatoa kwa jinsia nyingine kama jamii ya kibinadamu. Ila tunapaswa kujua hapa kwamba utii huu wa mke unaosisitizwa, ni kwa mume wake, na si amtii kila mwanamume. Mwili na viungo vyake ni mfano wa umoja katika kanisa la Kikristo kila kiungo ni muhimu na vinategemeana, kichwa, mapafu, au moyo haiwezi kusema wao ni wa muhimu kuliko mdomo, miguu, mikono au figo. Paulo anawaonya wazee wa kanisa kuhusu walimu wa uongo wanaofundisha injili ya uongo. Anawaonya wasiache upendo wao wa kwanza walipokuwa waumini wapya.

Roho Mtakatifu anatuwekea muhuri na kutupa uhakika wa wokovu wetu ili tusiwe na hofu ya kupotea. Kanisa lapaswa kuwa tofauti na dunia. Kristo ni mmoja, Roho mmoja, ubatizo mmoja, tumaini moja, imani moja na Mungu mmoja. Kwa neema tumeokolewa, kupitia imani, na si matendo yetu 2:20. Ni karama toka kwa Mungu, si kwa matendo yetu, wala awaye yoyote asije akajisifu. Paulo anawaambia watoto wawatii wazazi wao kama wamtiivyo BWANA, maana ni haki. Amri hii ndiyo ya kwanza yenye ahadi "upate kuwa na siku nyingi katika nchi upewayo na BWANA Mungu wako." Akina baba wanapewa wosia "msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya BWANA." Watumwa watii mabwana zao kwa hofu na kutetemeka.

Wale mabwana wenye watumwa nao wawatendee watumwa wao mema, na si kuwaogopesha na kuwanyanyasa; maana BWANA wa watumwa hao ni BWANA wao pia. Kwa Mungu hakuna upendeleo, mtu awe mtumwa au bwana mwenye watumwa, wote sisi tu watoto wa Mungu. Paulo anasema tutoe mambo yote ya ubinafsi, na matakwa yetu kama nguo chafu tuzivue na tuvae nguo mpya. Tusiwe watu wa magomvi na hasira. Isifike jioni na bado tuna hasira ya jambo fulani. Tuache njia zote za zamani mbaya kama wizi, uongo au kutotii wazazi na tufanye kazi ili tuweze kujitegemea na kuwa msaada kwa wengine. Tusiseme wengine vibaya. Daima tuchunge midomo yetu. Tuongee yale ya kusaidia, mawazo yetu yawe na kufikiria lililo bora. Yesu Ndiye amani na msingi wa kanisa lote. Twapasa kuwa nuru ya dunia tukienenda kwa upendo wote.

Paulo anamaliza barua yake kwa kutuambia kwa vile hatuwezi tukashinda wenyewe basi tuvae silaha Saba zote za Mungu ili tuweze kupinga hila za Shetani. Jambo hili ni muhimu zaidi leo kwetu tunaoishi mwisho wa historia ya dunia. Kila siku tupo

vitani, vita vipo mawazoni mwetu. Mapambano ya ufalme wa Mungu na ufalme wa Shetani. Kila dakika tunafanya maamuzi ya kumchagua Mungu au Ibilisi. Kwa maana vita vyetu si vya damu na nyama bali ni juu ya falme, mamlaka ya wakuu wa giza, juu ya majeshi ya mapepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Mafikarani mwetu yanapigana majeshi mawili, hivyo tuvae silaha. Tusimame hali tumejifunga Kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu ya utayari tupatao kwa injili ya amani. Tuvae ngao ya imani, ili tuweze kuizima mishale ya Shetani. Tena tuwe na chapeo ya wokovu na upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu. Tudumu tukisali na kukesha kila wakati tukidumu kuombea watakatifu wa Mungu wote duniani. Sala ndiyo silaha ya saba. Twaona askari hukingwa kila mahali kwenye mwili wake isipokuwa nyuma tu. Pengine hili ni fundisho kwetu, tukirudi nyuma kumtetea Yesu Kamanda wetu, adui ni rahisi kutuumiza, maana hatuna kinga yoyote.

Basi Yesu Kristo aendelee kukaa katika mioyo yetu. Yeye Ambaye ametuchukua kwenye familia yake ili tupate wote kufahamu jinsi ulivyo upana, na urefu na kimo na kina cha upendo Wake upitao ufahamu, kwa jinsi ulivyo kuwa mwingi.
Jitahidi sana kusali sala ya Waefeso 3 kila wiki! Nayo inasema hivi
"14 Kwa hiyo nampigia Baba magoti,
15 Ambaye kwa Jina Lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa,
16 Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho Wake katika utu wa ndani.
17 Kristo Akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo;
18 ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina;
19 na kuujua upendo Wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.
20 Basi Atukuzwe Yeye Awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;
21 naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina.

Wakati mwingine tunawekea mipaka kwa baraka za Mungu. Tunamwomba fadhila kwa uchache sana. Badala ya kuomba kwa wingi sana. Mungu anaweza na Yuko tayari kutubariki sana kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo! Ni wakati wa kuomba kama Yabesi, "Laiti ungenibariki kweli kweli!" Tusiweke vikwazo. Tusiweke kikomo. BWANA na akubariki leo, zaidi ya yote uyaombayo au uyawazayo! Bwana Awe Nasi, tuombeane.

*Katika Kristo kilio cha wanadamu kilimfikia Baba wa huruma isiyo na kikomo. Kama mwanadamu aliomba kiti cha enzi cha MUNGU hadi ubinadamu Wake ulichajiwa (ulipewa nguvu) na umeme wa mbinguni ambao ulifanya mwunganiko wa ubinadamu na Uuungu. Kupitia ushirika wa daima alipokea uzima kutoka kwa MUNGU, ili aweze kuupa ulimwengu uzima. Uzoefu wake unapaswa kuwa wetu wetu.
--------------------------------------

Maswali: Kwa nini watoto wanapaswa kuwatii wazazi wao? Kwa nini wanaume wanapaswa kuwapenda wake zao? Kwa nini wake wanapaswa kuwatii waume zao? Waajiri wanapewa wosia gani? Kwa nini watumishi wanapaswa watii mabwana zao? Silaha za Mungu ni zipi? Kwa nini watoto watii wazazi wao? Kwa nini watu wengi husema ingetokea hali ngumu na wangekuwa na uwezo wa kununua kitabu kimoja tu cha Biblia, basi wangechukua kitabu cha Waefeso. Jadili jinsi unavyoweza kuzivaa silaha za Mungu katika maisha yako ya kila siku. Sala hii ya Waefeso 3 inakupa picha gani?

**SIKU YA 333.**
**(Novemba 28)**

**Wafilipi.**

# Furahini katika BWANA tena nasema furahini



Filipi ndipo alipoishi Lidia, yule mfanya biashara wa nguo za zambarau. Na yule askari Jela aliyeongoka na familia yake wakaanza kanisa. Paulo alionyeshwa njozi usiku ya mtu amesimama akimsihi aje Makedonia kusaidia watu. Filipi ulikuwa mji wa Makedonia Ulaya. Watu wa mji huo, walimpenda na kumpa ushirikiano Paulo kuliko makanisa mengine. Epafrodito alikuwa msaidizi wa Paulo na rafiki wa Filipi, kisha akaenda Rumi kupeleka salamu toka Filipi, ila aliumwa sana, na baada ya maombi aliponywa na Mungu na akarudi Filipi na barua kwa waumini. Paulo anawashauri kwamba mtu awaye yoyote asiibe furaha yao!

Adui alitaka amtie Paulo gerezani ili akiwa gerezani amnyamazishe. Lakini barua zake alizoandika zikawa mbaraka kwa makanisa aliyosaidia kuanzisha na kwetu pia. Japo aliandika Wafilipi kifungoni, kitabu hiki kimezungumza neno furaha kama mara 20 hivi kwenye mafungu yake 104. Paulo Akijua kumwamini Kristo ni pamoja na kuteswa kwa ajili Yake, aliyahesabu mambo yote kama mavi tu yasiyo na faida ukilinganisha na uzuri wa Kristo (Wafilipi 3:8). Paulo anatuambia nasi kama washiriki wa Filipi, tusijisumbue kwa neno lolote bali katika kila neno kwa kusali, kuomba na kushukuru, huku haja zetu zikijulikana na Mungu. Na amani ya Mungu ipitayo akili za binadamu itatuhifadhi mioyo yetu, na nia zetu katika Yesu Kristo.
Filipi ilikuwa chini ya milki ya Rumi, hivyo waliweza kumsaidia kwa namna nzuri mahitaji yake mtume Paulo kule gerezani. Paulo hakupenda kupokea msaada wa pesa kutoka kwa watoto wake katika imani, maana hakutaka awape mzigo, akisema

yeye kama baba ndiye anawajibika na jukumu kuwasaidia watoto. Paulo alikubali zawadi za Filipi kama mahusiano yao ya pekee, akijua wanatoa vyao kwa dhati kabisa, na kwa upendo mwingi. Hata leo tukifika mahali mtu aweza kutulazimisha tule, au kutupa kitu kwa dhati au kwa kutujaribu tu, huku akitaka tukatae ili abaki na vitu vyake. Hebu leo tutoe bila ya uchoyo, au kinyongo.

Paulo anasisitiza Yesu ni Mfano wa pekee na wa ajabu wa sisi waumini. Yeye ni Mfano wa kuigwa kwani alikuwa pamoja na Baba Yake mbinguni, ila aliacha utukufu Wake wote, na kwa unyenyekevu akaja kukaa nasi, na kutendewa uovu kwa ajili yetu. Alijidhili japo alikuwa Mungu, na kuwa mtumwa. Anatusihi "tuwe na nia iyo hiyo ndani yetu ilikuyokuwa ndani ya Kristo Yesu." Nia ya kufanya vitu bila ya kutaka kuonekana, kulipwa au kusikia kiburi. Mungu akamwadhimisha Yesu na kumpa Jina Lipitalo majina yote, na kila goti litapigwa mbinguni na duniani kwa Jina hili la Yesu. Na kila ulimi utakiri YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu BABA. Tunaomba tumkiri tukiwa washindi, na sio wale walioshindwa.

Anatukumbusha kuushughulikia wokovu wetu kwa kuogopa na kutetemeka. Ni furaha iliyoje kwamba Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwetu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu. Tuwe tayari kumwamini hata kuteswa kwa ajili Yake. Mungu atusaidie ili tusije kuonekana wenye haki yetu wenyewe bali haki Yake. Haja yetu kubwa ni tuweze kumjua Yeye na uwezo wa kufufuka Kwake na ushirika wa mateso Yake. Japo wengine wamhubiri Yesu kwa wivu, au fitina na wengine kwa nia njema au upendo, ilimradi katika njia zote kwa hili na kwa Kweli, Yesu anahubiriwa. Paulo hajidhanii kwamba ameshafika au ameshajiwezea bali anatenda neno moja tu "anasahau yaliyo ya nyuma na kuchuchumilia yaliyo ya mbele, anakaza mwendo afikie ile medali au taji ya thawabu ambayo Kristo Yesu atampa." Nasi ndiyo liwe goli letu leo; kuichuchumilia ile medali ambayo siku moja Kristo atatupa.

Tujifunze kuridhika, na kuwa radhi na hali yoyote, katika kufanikiwa katika njaa, katika kuwa na vingi na katika kupungukiwa. Maana utauwa na kuridhika ni faida kubwa, tulikuja duniani bila kitu, hata nguo hatukuzaliwa nayo. Na mtu akifa hachukui chochote na kwenda nacho kaburini. Mungu Ndiye anatuwezesha na kututia nguvu siku kwa siku. Anawashukuru washiriki wa Filipi kwa kumtuma Epafrodito kumletea pesa ya kutumia. Asema kuishi kwake ni kwa ajili ya Krito na kufa ni faida kwa kazi ya Mungu kwani alikuwa gerezani kwa ajili ya Kristo. Paulo anasema hataki kujipotezea muda na mambo mengine isipokuwa kumjua Kristo tu. Anataka Wafilipi waishi kila siku wakingoja ujio wa Yesu.

Paulo anafurahi kwamba injili inahubiriwa, anafurahi kwamba anapata mateso; anawaambia wengine pia wafurahi, anasema kanisa la Filipi ni furaha na taji yake. Anawaambia "furahini katika BWANA tena (nasema) furahini." Huu ni wimbo mzuri, hebu imba! Kwa sababu tunaishi dunia yenye shida, tunarudia "tusijisumbue na kujichosha na mahangaiko au matatizo yanayotupata bali kwa kila neno tusali, tukiomba na kushukuru. Haja zetu zote tulizo nazo tumjulishe Mungu; tusimfiche, japo anajua kwamba tuna shida hizo, kwa kumwambia, tunampa nafasi au uchaguzi wetu, ili atufanyie makuu kwa kadiri ya juu ya mamlaka Yake."

Kisha kinakuja kile kichujio cha kila kitu katika maisha yetu "Hatimaye ndugu zangu, mambo yoyote yaliyo ya Kweli, yaliyo ya staha, yaliyo ya kupendeza, yaliyo ya sifa njema, yaliyo ya sifa nzuri, tutafakari hayo." Fungu hili ni la kukariri. Maaana ndiyo rula au kipimo/kiwango chako na changu kabla ya kufanya lolote, iwe ni kuimba, kutembea, kuvaa nguo, shahada, taaluma, mchezo, uchumba, urafiki, ununuzi wa bidhaa,  kula au kufanya lolote jiulize swali hili. Mfano: kitabu ninachosoma, nyimbo ninayoimba, au program ya TV ninayoangalia, Je, ina Ukweli? Ina staha? Inapendeza? Ina sifa njema? Ina sifa nzuri?  Kama ni jibu ni la! usisome, au kuimba au kuangalia program hiyo. Kama ni ndiyo basi imba, soma au uangalie program hiyo.

Paulo aliwatia moyo Wafilipi kusimama imara katika Bwana na hii inatuhusu sisi pia. Njia ya kusimama imara ni kuweka macho yetu kwa Kristo, na kukumbuka kwamba ulimwengu huu sio makao yetu. Hakika  ni ajabu kwamba mtu aliye gerezani  analiambia kanisa lifurahi. Lakini mtazamo wa Paulo unatufundisha somo muhimu: mitazamo yetu ya ndani si lazima iakisi hali zetu za nje. Paulo alijawa na shangwe kwa sababu alijua kwamba haijalishi ni nini kitampata, Yesu Kristo alikuwa pamoja naye. Ni rahisi kuvunjika moyo kuhusu mambo yasiyotupendeza au kuchukua matukio yasiyo muhimu kwa uzito upitao kiasi. Hatimaye furaha hutoka kwa Kristo ikae ndani yetu. Kristo Yu karibu, na katika kuja Kwake mara ya pili tutatambua kwa utimilifu furaha hii kuu. Yeye anayeishi ndani yetu atatimiza makusudi Yake ya mwisho kwa ajili yetu. Baada ya muda kidogo akina kaka na dada, tutakuwa tukienda nyumbani! Hebu tushangilieni!

Haitoshi kusikia au kusoma Neno la Mungu, au hata kulijua vizuri. Ni lazima pia tuweke katika vitendo. Je, tunavaa nini, ni miziki gani tunasikiliza, marafiki zetu ni nani, Je, tunachukua muda kwaajili ya ibada? Hakika tunaweza kumtumainia Mungu kwamba atatimiza mahitaji yetu daima. Chochote tunachohitaji duniani Yeye atatupatia siku zote, hata kama ni ujasiri wa kukabiliana na kifo kama Paulo alivyofanya. Ila ni lazima tukumbuke  kutofautisha kati ya matakwa yetu na mahitaji yetu.

*"Jitengeni ninyi wenyewe," anatualika. Ikiwa tutatii Neno Lake, tunapaswa kuwa na nguvu na wenye manufaa zaidi. Wanafunzi wakamtafuta Yesu, wakamwambia yote; na Akawatia moyo na kuwafundisha. Ikiwa leo tutatenga muda kumwendea Yesu na kumwambia mahitaji yetu, hatupaswi kukatishwa tamaa (au hatutadondoshwa).
--------------------------------

Maswali: Barua hii iliandikwa wapi? Kwa nini inaitwa barua ya furaha? Nia ya Kristo ni ipi? Kwa nini Paulo anasahau ya nyuma? Kwa nini kuridhika ni muhimu? Tunaambiwa hatimaye tutafakari mambo gani? Kichujio kikubwa cha maisha yetu kinapaswa kuwa kipi?

**SIKU YA 334.**
**(Novemba 29)**

**Wakolosai.**

# Kama tulivyompokea Kristo tuenende vivyo hivyo katika Yeye.



Hatujui injili ilivyofika Kolosai pengine kupitia miji mingine. Thesalonike ulikuwa mji mkubwa wenye bandari, katika Makedonia ya Uyunani. Washiriki wengi hapa walikuwa wapya na watu wa mataifa. Paulo anawaandikia wosia wa kuishi maisha ya kumcha Mungu. Epafra wa Kolosi alikuwa mtumishi na rafiki wa Paulo katika injili. Barua hii yasema mafundisho ya uongo yalianza kuingia kwenye kanisa, pengine kupitia mkanganyiko wa mafundisho. Huyu alimwambia yale matatizo yanayoendelea katika kanisa la Kolosai. Barua hii pengine iliandikwa pamoja na ile ya Waefeso na Filemoni. Mafundisho ya uongo yalikuwa yameingia, na Paulo anachukua muda kuwaelezea kwamba Yesu anatosha kwa maisha yetu, kwa kupata wokovu, kutuombea na kutakaswa. Yesu na si wanajimu, wachawi au wabashiri ndiyo njia ya Kweli na uzima.

Yesu Kristo alikuwa wakala ambaye kupitia kwake Uungu uliumba kila kitu mbinguni na duniani. Hawa ni pamoja na malaika na Lusifa ambaye alifanyika Shetani, na ambaye alimsulubisha Kristo msalabani. Kwamba Yesu angeruhusu mtu Aliyemuumba ampigilie misumari msalabani ili kuokoa wanadamu inaonyesha upendo wa ajabu alionao kwa wanadamu. Mungu atusaidie kuuona upendo huu wa kutosha ili tuuitikie kwa kumpenda kwa moyo wetu wote, roho zetu zote na akili zetu zote.

Yesu ni Mungu, Picha ya Mungu anayeonekana, mzaliwa kwa kwanza wa viumbe vyote, kwa kuwa katika Yeye vitu vyote viliumbwa vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi vinavyoonekana na visivyookenana ikiwa ni vitu vya enzi au usultani au mamlaka, vitu vyote viliumbwa kwa njia Yake na kwa ajili Yake. Yesu amekuwako

kabla ya vitu vyote. Yeye ndiyo kichwa cha mwili wa kanisa. Yeye ni Mwanzo na Mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote. Yeye ni mpatanishi kwa kumwaga damu Yake msalabani. Hivyo tuwe macho mtu yoyote asitufanye kuwa mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu kwa jinsi ya mapokeo ya mwanadamu na mafundisho ya ulimwengu yasiyo ya Mungu.
Tuvae rehema, utu wema, unyenyekevu, upole na uvumilivu tukichukuliana na kusameheana bila kulaumiana kama BWANA anavyotusamehe sisi. Tujivike upendo ndiyo kifungo cha ukamilifu. Paulo alitaka tujue kwamba hatuwezi kushika sheria kwenda mbinguni, ni Yesu peke Yake anatupa uzima wa milele. Anawakumbusha waumini wa Kolosai wakumbuke yale walifundishwa na Epafrasi, mwanzilishi wa lile kundi, kama walivyompokea Kristo Yesu waende vivyo hivyo katika Yeye na kujengwa katika Yeye wakiota mizizi ili wawe imara. Tudumu katika kuomba, tukikesha na shukrani, na tukiombea watenda kazi wa Mungu ili milango ifunguke katika kuhubiri Neno Lake. Paulo anawashauri washiriki waimbe Zaburi, nyimbo za kiroho na tenzi.

Hata Mungu anaimba pia Zefania 3:17. Nyimbo ni sehemu muhimu ya maisha ya muumini. Martin Luther Mchungaji wa Ujerumani akifanya matengenezo ya imani na Maandiko alifanya matengenezo ya nyimbo pia. Watu wengi wamepata ujumbe kupitia nyimbo, yapasa tuimbe nyimbo zenye Kweli ya Neno la Mungu, maana kuna nyimbo zenye mafundisho ya uongo na midundo ambayo inapeleka mawazo yetu kwenye nguvu za giza au tamaa za mwili. Nguvu ya Wimbo kwa maadili haiwezi kusemwa jinsi ya kutosha. Historia ya nyimbo za Biblia imejaa mapendekezo kuhusu matumizi na manufaa ya muziki. Muziki mara nyingi hupotoshwa ili kutumikia makusudi ya uovu, na hivyo huwa mojawapo ya wakala wenye kuwavuta watu kwenye majaribu na hata dhambi. Lakini, ikitumiwa ipasavyo, ni zawadi ya thamani ya Mungu, iliyokusudiwa kuinua mawazo kwenda kwenye mada ya juu ili kumtia mtu moyo na kuinua roho. Wana Israeli waliimba nyika. Malaika waliimba walipokuwa wakiwapa watu habari kuhusu kuzaliwa kwa Yesu. Kuimba ni tendo la ibada, hakuna kinachosaidia moyo kama kumsifu Mungu. Nyimbo ni silaha dhidi ya huzuni na kukata tamaa. Twaweza kufanya kazi kwa furaha tukiimba na kumtukuza Mungu. Muziki unatusaidia kujifunza Maandiko kwa njia rahisi pia!
Anatukumbusha wote Twende kwa hekima tukiukomboa wakati. Maneno yetu yawe na neema siku zote, yakiwa yamekolea viungo vizuri, tupate kujua jinsi ipasavyo kujibu kila mtu. Si kwa kuropoka ropoka, tukishushua watu na kuwavunja watu moyo, au kuwatia huzuni, bali kwa hekima. Mawazo yetu na maneno yana mahubiri makubwa.

Tujihadhari na mafundisho yasiyo ya kweli. Ukristo ni mtindo wa maisha, ni mahusiano ya familia ya Mungu, na si dini tu. Katika maisha yetu ya kila siku shuleni, nyumbani, kazini na kwenye jumuiya; Tuyaweke mawazo yetu kwa vitu vya mbinguni, tuweke mbali hasira, ghadhabu, uovu, matukano, matusi, na uongo. Kusiwe na Myahudi au Myunani, mgeni au mwenyeji, mtumwa au mwungana, tajiri au masikini, mweusi wala mweupe, mfupi wala mrefu, mnene wala mwembamba, bali Kristo katika yote. Anakazia tena kama barua ya Waefeso kwamba wake wawatii waume zao kama inavyompendeza BWANA. Mke anayemkosea mume wake heshima anamwangusha Yesu, na kufanya watoto wawe na tabia mbovu.

Wanaume wawapende wake zao kwa dhati bila kuwachukia au kuwa na uchungu nao, kisha wasiwe wakatili kwao. Watoto watii wazazi wao, maana jambo hili lampendeza BWANA. Ni mahubiri makubwa kwa waumini na zaidi, kwa watu wasiomjua Mungu endapo wakina baba, wakina mama na watoto watafuata maagizo haya. Haya si maagizo rahisi ila tuombe Mungu tuyafanye kwa upendo. Anawasihi wakinababa wasichokoze watoto wao wasije kuwakatisha tamaa. Mtu anayemchokoza mtoto ili apate hasira au kumkejeli kwa hila mbaya, mara nyingi anakuwa hajakomaa kiakili. Hebu tuache uovu huu. Watumwa wawatii mabwana zao katika mwili, wakimcha BWANA. Lolote tufanyalo tufanye kwa moyo kama tunamfanyia BWANA. Tukijua tutapokea urithi wa kumtumkia Kristo Yesu.
Wengi wana watenda kazi wa nyumbani au ndugu wanaowasaidia; iwe ni yaya, shamba boi, dereva, dobi, mpishi, au kibarua fulani. Jiweke kwenye viatu vyao. Tulipokuwa watoto tuliona hata watoto wengine wakikashifu watenda kazi wanaofanya majumbani mwao kwa matusi na kuwafanyia hiyana. Hili liwe mwiko kwa mtoto au mtu ampendaye Mungu. Watumishi wetu wafanye kazi kwa masaa na kupumzika, walipwe haki zao bila dhuluma, na kutendewa kwa upendo kama vile tunavyomtendea Yesu. Tuwe na upole, uvumilivu, tukisameheana na wenzetu kama BWANA alivyotusamehe sisi. Basi tukumbuke tena "Neno la Kristo likae ndani yetu, tukifundishana na kuonyana kwa Zaburi, nyimbo na tenzi za rohoni huku tukimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwetu.

Kila tendo tufanyalo tulifanye kwa Jina la BWANA Yesu. Tukifikiri yaliyo juu mbinguni na siyo yaliyo chini, tukidumu kuomba usiku na mchana na kumshukuru Mungu na kuukomboa wakati, tupae kujua Yesu yu mlangoni, lolote tufanyalo tufanye kama tunamfanyia BWANA na si binadamu." Tikiko alichukua barua hii Kolosai.

Ni fursa nzuri jinsi gani kumpenda, kumtumikia na kumtii Yesu. Mungu atusaidie tudumishe uaminifu usio na mgawanyiko na uaminifu Kwake.

*Kwa mtenda kazi aliyejiweka wakfu kuna faraja ya ajabu katika kujua kwamba hata Kristo wakati wa maisha Yake duniani alimtafuta Baba Yake kila siku kwa ajili ya ugavi mpya wa neema iliyohitajika; na kutokana na ushirika huu na MUNGU alienda kuwaimarisha na kuwabariki wengine.
-------------------------

Maswali: Yesu ni nani? Kwa nini watoto watii wazazi wao? Kwa nini wanaume wasikasirikie wake zao? Kwa nini wake wanampendeza BWANA wakitii waume zao? Kwa nini ni muhimu kuachana na magomvi na mabishano yasiyo na maana? Twawezaje kuwahuzunisha watu wanaofanya kazi majumbani mwetu? Kwa nini ni dhambi kutesa watumishi au watenda kazi? Kwanini ni vibaya kutomtii mkubwa wako wa kazi au kuleta chokochoko na hiana` kwenye nyumba uliyoajiriwa?

**SIKU YA 335.**
**(Novemba 30)**

**Wathesalonike.**

# Tuombe bila kukoma



Mji wa Salonika au Thesaloniki upo Uyunani. Paulo anawashukuru waumini kwa imani na upendo wao kwa Mungu anatamani awatembelee na anawaombea kwa mateso wanayopata na kuwaambia waumini waishi maisha ya utakatifu kwa Yesu Kristo. "Twamshukuru Mungu siku zote kwaajili yenu nyote tukiwataja katika maombi yetu, injili haikuwafikia kama maneno tu bali katika nguvu, na katika Roho Mtakatifu." Paulo anawasifu kwamba imani yao imeenda kote jinsi walivyomgeukia Mungu aliye hai na kuacha sanamu, na sasa wanamngoja Yesu aje mawinguni. Paulo asema kuingia kwao kuhubiri huko hakukuwa bure. Thesalonike ilikuwa bandari yenye shughuli nyingi, hasa za kibiashara. Paulo aliwaambia wasomaji wake waishi maisha ya utauwa na usafi. anawakumbusha juu ya ujio wa pili wa Yesu.

Ni muhimu kutambua kwamba uhusiano wao haukuishia kwa Wathesalonike. Baada ya kumfuata Paulo, bali wao wakawa "kielelezo kwa waamini wote katika Makedonia na Akaya". Wafuasi hawa walikuwa viongozi baadaye. Wale ambao walikuwa wamefundishwa wakawa washauri kwa wengine. Paulo anasisitiza kwamba zawadi ya wokovu ni mwanzo tu wa safari yetu ya kiroho; mara tunapomwamini Kristo, tunaitwa kukua katika imani, tumaini na upendo.

Paulo anawaambia washiriki kwamba wao kama wahudumu katika Kristo, hawakutafuta utukufu wa mwanadamu kwao, au kwa wengine, hawakuwalemea kama mitume, bali walikuwa wapole katikati yao kama vile mlezi awatunzavyo watoto wake mwenyewe." Anawaombea wafanywe imara mioyo yao iwe bila lawama katika kutafuta utakatifu mbele ya Mungu BABA yetu wakati wa kuja Kwake BWANA wetu Yesu pamoja na watakatifu wote. Paulo anamshukuru Mungu bila kukoma. Anashauri wote tuombe bila kukoma. Kuomba huku ni kule rasmi na kule kusiko rasmi (structured and unstructured), ukiwa umelala, ukiwa unatembe, ukiwa umesimama unangoja basi na ukiwa umepiga magoti kwenye maombi yako ya faragha. Soma kitabu cha Nuku cha maombi ambacho tumetafsiri. Maombi ya

hadhara yasiwe marefu maana huwavunja moyo wengine. Siri ya ushindi ni maombi ya faragha. Kubwa katika maombi ni kuomba mba kwa dhati, ari na bidii, maombi yasiyo ya desturi au feki. Washiriki wapya wa Thesalonika walitegemea kwamba Yesu atarudi mara ya pili na kuwakuta hai. Walipoona kwamba wenzao wanaanza kufa au kulala usingizi wa mauti walipata mshangao na kufa moyo, maana walidhani wataishi mpaka Yesu awarudie tena mawinguni. Hofu hii imekumba kila mtu leo, maana hakuna anayeponyoka kifo. Paulo aliona awaeleze kuhusu kifo ni nini maana wangeona ni kujipotezea muda tu kumwamini Yesu.

Kumtumaini Mungu na Neno Lake kuhusu ufufuo si ndoto za mchana, bali jambo halisi litakalotokea. Ujasiri wetu kwa yale Mungu atakayofanya siku za mbele na kutufufua; unatokana na yale tunayoona anafanya katika maisha yetu sasa. Paulo anawaambia watu waliokufa watafufuliwa na kuwa na Yesu atapokuja mara ya pili "Lakini ndugu hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika, kama wengine wasio na matumaini. Maana twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja Naye…sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja Kwake BWANA, hakika hatuwatangulia wao waliokwisha kulala mauti, kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya Malaika mkuu na parapanda ya Mungu nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza, kisha sisi tulio hai tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu tumlaki BWANA hewani, na hivyo tutakuwa pamoja na BWANA milele."

Basi tufarijiane kwa Maneno haya ya hakika. Paulo aliendelea kuzungumza zaidi kuhusu kifo akiwaandikia Wakorintho, akasema itakuwa kama umeme na radi. Watakatifu watasikia sauti ya Mwana wa Mungu akiita watakatifu waliokufa "amkeni, amkeni." Wafu wote walio makaburini watasikia sauti Yake, na watafufuka. Masikini, wafungwa, wanene, wafupi, matajiri na masikini, wote miili yao ya kuharibika itavaa kutoharibika au kutokufa ndipo watakaposema "mauti imemezwa…kuwa wapi ewe mauti kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?" Yesu atakuja kurudisha kilichopotea. Je, tufanye nini tukingojea haya yote? Mtu akifa kutokana na Maandiko haendi mbinguni papo hapo, na ndiyo maana makaburi yatafunguka na wafu watatoka humo kumlaki Yesu. Roho haiwezi kukaa yenyewe bila mwili. Nafsi hai au mtu ni roho au pumzi ya uhai na mwili. Mwili hauwezi kuwa pekee yake na akawa mtu, au roho yaani pumzi ya uhai haiwezi ikaishi yenyewe bila mwili na kuitwa mtu.

Paulo anazungumzia imani, matumaini na upendo. Anatuambia kama Yesu alifufuka basi nasi tusiwe na shaka maana ni tumaini la baraka ambalo Kristo Mwenyewe Ambaye ni ufufuo na uzima atatupa. Akawatia moyo waumini kuhusu kuja kwa Yesu mara ya pili. "Siku ya BWANA yaja kama vile mwizi anavyokuja bila ya kusema kwamba aja, watu wasemapo kuna amani na salama ndipo uharibifu uwajiapo ghafla kama uchungu umjiavyo mama atakaye kujifungua, bila kutegemea. Ila sisi hatumo gizani, hata siku hii itupate kwa ghafla kama mwizi ajavyo nyumbani mwetu. Maana sisi tu wana wa nuru, na wana wa mchana si wanaofungwa na giza wasijue litakalotokea. Tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe na kuwa na kiasi, tukijivika kifuani imani na upendo, na chapeo ya tumaini la wokovu. Tuwe na Kristo

tukifarijiana kwamba twakesha au twalala tukijengana kila mtu na mwenzake. Mkono mmoja kwa imani ukimshika Yesu, na mkono mwingine ukiendesha shuguli zetu za kila siku hapa duniani.

Anakazia tena, wafurahi na kuomba bila kukoma, wakishukuru kwa kila jambo, wahifadhiwe wasiwe na lawama, wakati wa kuja BWANA. Anawakumbusha, ni Mapenzi ya Mungu katika Kristo, wasimhuzunishe Roho wa Mungu, washike yaliyo mema na kujitenga na ubaya wa kila namna. Barua hii na ya Wakorintho imejibu maswali ya kila muumini ya kifo ni nini, na kwamba Yesu atakapokuja itakuwaje. Watu watafufuka wakiwa na miili na siyo roho zinazoelea kwenda mbinguni.

*Maombi Yalimtia Nguvu Yesu kwa Ajili ya Majaribu—Kristo Mwokozi wetu alijaribiwa katika mambo yote kama sisi, lakini hakuwa na dhambi. Alichukua asili ya mwanadamu, tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, na mahitaji Yake yalikuwa mahitaji ya mwanadamu. Alikuwa ana mahitaji ya kimwili yaliyohitaji kutimizwa, uchovu wa mwili uliopaswa kuondolewa. Ilikuwa ni kwa maombi kwa Baba Yake ndipo alipoandaliwa na kuimarishwa kwa ajili ya wajibu na kwa majaribio. Siku baada ya siku Alifuata mzunguko Wake wa wajibu, akitafuta kuokoa roho. Naye akakesha usiku kucha akiomba kwa ajili ya wale waliojaribiwa.
-------------------------

Maswali: Waliokufa katika Yesu watafufuka kwa ufufuo wa uzima ina maana gani? Kwa nini ni muhimu kuweka macho yetu kwenye medali Yesu atatupa kuliko kitu chochote? Siku ya BWANA yaja kama mwivi ina maaga gani? Kushukuru au kuomba bila kukoma ina maana gani?

**SIKU YA 336.**
**(Desemba 1)**

**Wathesalonike wa pili.**

# Asiyefanya kazi na asile.



Madhumuni ya kuandika kitabu hiki ilikuwa ni kuwafariji watu na kuwatia moyo wakati wa mateso. Kama simu ingalikuwepo, pengine ingepunguza shida hizi, kwani kungekuwa na mawasiliano ya mara kwa mara! Katika barua ya Pili Paulo anatazamia matokeo mema ya kazi yake kwa Wathesalonike. Wakati wa Ujio wa Pili, waamini wataokolewa kutoka kwa watesi wao kwa msaada kutoka kwa Mungu katika Kristo ( 1:5-10 ). Lengo la Paulo katika fungu hili si kufurahia kisasi ( 1:8-9 ), bali ni kuwatia moyo walionyanyaswa na kuonewa ( 1:5-7 ). Ujio wa Pili utawawezesha Wathesalonike kuwa "pamoja na Bwana." Hapo watesi wao watafukuzwa mbele za uso wa Bwana, si kwa sababu Yeye anawachukia, bali ni kwa sababu tabia zao haziwezi kustahimili uwepo wa utukufu wa Mungu. Makanisa mengi ya magharibi au yale yanayozungumza kingereza hayajapata shida hiyo ya mateso siku za karibuni. Paulo anashukuru kanisa linaendelea kukua japo kulikuwa na mateso kwa watu wa Mungu. Paulo anatuma maonyo kwa wale wavivu ambao wana mtazamao usio mzuri. Wengine wameacha kazi na kukaa kivivu wakitegemea Yesu anarudi hivyo hamna haja ya kufanya kazi. Paulo anasema wasiwatumie

Wakristo wengine kuwatimizia mahitaji yao, maana hiyo ni sawa na kuwadhulumu wengine.

Binadamu aliambiwa atakula kwa jasho, hivyo Paulo anaagiza waumini hawa wavivu watengwe na washiriki wengine, ili waweze kutubu. Ila wakaribishwe tena kama ndugu, kama wametubu. Uvivu ni kitu kibaya mno. Hapa mtume anaandika maneno mazito akisema "ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi asile chakula." Wavivu wapaswa wale chakula chao wenyewe, si kuranda randa miji ya watu na kudoea vyakula vya watu na hali wana nguvu zao na uwezo wa kulima. Au kufanya vishuguli vidogo vidogo vya kivivu wakati ambao waweza kufanya makubwa na kujisaidia, au hata kusaidia wengine. Na wengi wana ardhi, ila hawaitumii. Yeyote mwenye ardhi hawezi kufa na njaa, mpango wa Mungu kwa Israeli ilikuwa kila mtu awe na ardhi ili kusiwe na umasikini. Tabia ya watoto wanaofundishwa mpango wa maandiko vijijini ni mara kumi bora kuliko watoto wanaolelewa mijini. Hebu kila mtu ajue kulima, kufanya kazi kwa ustadi na kujitafutia riziki na siyo kukaa mjini au kijijini bila kazi.

Kazi ni muhimu hata kama ni kazi za nyumbani, iwe kufagia, kulima, kudeki, kupasi, kusafisha madirisha, kuosha mifugo, kuosha vyombo, kuchunga mifugo, kupika, kukata miti, kulima mashamba na zingine. Kila mtoto anapaswa ajifunze kazi. Angalia chati ya umri gani na kazi gani kwenye mtandao, na kisha upangie uone ile kazi unayoweza kuifanya. Mbali na kumwamini Mwenyezi Mungu na Mwana Wake Pekee Yesu Kristo, kinachofuatia kwa umuhimu ni kufanya kazi. Kazi ilitolewa na Mungu hata kabla ya maanguko ya binadamu katika dhambi. Mtu alipewa kazi hata kabla ya ndoa! Paulo anasema maombi ni muhimu ili kupata nguvu za Mungu, kushinda au kuvumilia majaribu. Paulo anasema imetupasa kumshukuru Mungu siku zote kwajili ya waumini, kwa kuwa Mungu ametuchagua mwanzo katika kutakaswa na Roho.

Paulo anazungumzia siri ya kuasi ya 'mpinga Kristo' anayejiinua nafsi yake kwa kila kiitwacho Mungu, na kuabudiwa, akitaka awe Mungu "maana ile siri ya uasi inatenda kazi." Watu wanaompinga Kristo wataangamizwa na Pumzi ya kinywa cha Mungu. Hata wale wadhalimu na wanaopotea kwa sababu ya kutopenda kuikubali ile Kweli, watahukumiwa. Paulo anasema kila mtu aende kwa utaratibu, na wala si kwa kufuata mapokeo. Tusiishi maisha ya kiholela, bali tuwe na mpango, hata wa kuandika mambo fulani ili tusisahau, kusoma Neno la Mungu, iwe kazi za nyumbani, za shule au majukumu mengine.

Je tufanyeje basi tunapoishi duniani leo? Jibu mtume anasema, "Kwa hiyo wapenzi kwa kuwa tunatazamia mambo hayo ya mbingu mpya na nchi mpya ambayo haki yakaa ndani Yake basi tufanye bidii ili tuonekanae katika imani kuwa hatuna mawaa wala aibu mbele Zake. Yabidi tuwe watu ambao tuna kiu ya kutafuta haki, tuwe wapole, wenye rehema, wapatanishi na watu ambao tunampenda Mungu kwa mioyo yetu yote, akili, roho na nguvu na jirani kama nafsi zetu. Yesu alikuja kuishi maisha ya kuhudumu wengine na kutumika. Hivyo ombi kubwa tukingoja siku ya kuja kwetu, ni "TUWE KAMA YEYE yaani TUFANANE NAYE."

Paulo aliandikiwa na makatibu muhtasi wake, wale aliokuwa akifanya kazi nao mara nyingi ila barua chache kama hii aliandika mwenyewe akisema mwishoni "salamu zangu mimi Paulo, kwa mkono wangu mwenyewe, hii ndiyo alama katika kila waraka, ndiyo mwandiko wangu. Neema ya BWANA wetu Yesu Kristo, na iwe pamoja nanyi nyote. Mawasiliano na watu ni mbaraka mkubwa, iwe kwa simu, kuzungumza uso kwa uso, au kwa barua. Hebu fanya kazi yako kama mtu anayengojea ujio wa Yesu wa mara ya pili, na ambaye anataka Yesu amwambie atakapokuja: "Vema, mtumishi mwema na mwaminifu; umekuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi. Ingia katika furaha ya Bwana wako." Mathayo 25:23

*Majira ya usiku ya maombi ambayo Mwokozi alitumia mlimani au jangwani yalikuwa muhimu kumtayarisha Yeye kwa ajili ya mitihani ambayo ilikuwa lazima akutane nayo katika siku zijazo. Alihisi hitaji la kuburudishwa na kutiwa nguvu rohoni na mwilini, ili aweze kukabiliana na majaribu ya Shetani; na wale wanaojitahidi kuishi maisha Yake watahisi hitaji hilo hilo.


---

Je, kwako wewe njia bora ya kuwasiliana ni ipi? Maswali: Kwa nini mtu asiyefanya kazi asile? Je wewe una kazi gani unazozifanya au kusaidia kila siku? Je Yesu alikuwa na kazi gani alipoishi duniani? Kwa nini ni muhimu kuwa na utaratibu na mipangilio katika shughuli? Paulo mwenyewe alifanya kazi gani? Mpinga Kristo ni nani? Kufanana na Yesu ina maana gani?

**SIKU YA 337.**
**(Desemba 2)**

**Timotheo wa kwanza.**

# Tabia ya Mchungaji na Shemasi.




Barua za Paulo ni zaidi ya nusu ya Agano Jipya. Paulo alimwandikia Timotheo barua ya kichungaji. Barua za Timotheo na Tito ni barua za viongozi wa kanisa hata leo. Timotheo anaambiwa jinsi anavyopaswa kufanya kazi kama mchungaji au mtumishi wa Mungu. Anaelekezwa mwenendo wa wachungaji na mashemasi, unavyopaswa kuwa. Maneno yao, mawazo yao, nia zao na mafikara yao. Timotheo muumini toka Efeso, Lysta, alizuru na Paulo kwenye ziara zake za kutembelea makanisa. Paulo aliiandika barua hii wakati Paulo aliachiliwa kifungoni kwa muda.
Timotheo alipata injili kwa mama yake Yunia, na nyanya yake Loisi. Baba yake alikuwa Mgiriki. Kanisa la Efeso lilikuwa linaingiza mafundisho ya uongo ya gnosticim yaani kuabudu miungu zaidi ya Mungu wa mbinguni. Watu wengine waliona wanajua mambo mengi kuliko wengine hivyo ni bora. Walikuwa wanachukua muda kuzozana, na kuleta magomvi, watu wakaanza kutoaminiana. Mafundisho haya yalitenganisha mwili na roho, kwamba mwili una uovu, ila roho ndiyo ina misimamo na mambo ya kiroho. Paulo akamwambia Timotheo abakie Efeso kusaidia kuondoa mafundisho haya na kuleta nidhamu kwenye makanisa anaambiwa jinsi ya kuchagua viongozi wazuri na kuweka mfano mwema wa kuigwa. Anapewa wosia jinsi ya kuwasaidia washiriki wenye shida, na kuwaonya wasifundishe elimu nyingine.

Paulo anashukuru kwamba japo mwanzo alikuwa mtu wa Jerui, mtukanaji na wa kuudhi watu, rehema ya Mungu imemsaidia, kwa kuwa alitenda kwa ujinga, kwa kutojua alichokifanya. Anasema “Ni Neno la kuaminiwa kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni atuokoe sisi sote wenye dhambi, ambao wa kwanza wao ni mimi.”
Paulo amwambia Timotheo, watu wote watoe dua, wasali, waombe na wadumu katika shukrani. Anasema Mungu ni mmoja tu na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja tu, Naye ni Yesu Kristo. Anasema watu wasalipo wainue mikono iliyotakata, na wanawake wajipambe kwa kwa adabu, na moyo wa kiasi, si kwa kujionyesha walivyosuka, wala kuweka dhahabu, lulu au vitu vya thamani. Bali wamche Mungu. Mwanamke asiwe juu ya mwanamume bali awe mtulivu, kwa

kuwa Adamu aliumbwa kwanza kisha Hawa.

Anasema mtu akitaka kazi ya uchungaji au uaskofu afanya vyema ila awe mtu asiyelaumika, mwenye mke mmoja tu, awe na busara, kiasi, mkaribishaji, ajuae kufundisha, mtu asiyetumia pombe, na mpole. Si mwenye mabishano, asiwe mwenye kupenda fedha, anayesimamia nyumba yake vyema, na kutiisha watu wa nyumbani mwake wawe na adabu. Maana kama hajui kusimamia nyumba yake yenye watu wachache, atasimamiaje nyumba ya Mungu. Asiwe mtu aliyeongoka karibuni, kwani atajivuna, kisha imepasa awe mtu aliyeshuhudiwa na watu vizuri.

Vivyo hivyo shemashi awe na tabia hizo hizo zilizotajwa kwa mchungaji. Ashuhudiwe mema, asinywe pombe, asiwe msingiziaji, awe mstahivu, asiwe ndumila kuwili, na asitamani fedha ya aibu. Watenda kazi hawa wajaribiwe kwanza, wakisha kuonekana hawana hatia watumike. Mtu akifanya kazi hii vyema, itakuwa mvuto mwema kwenye jumuiya. Asiwe msengenyaji, ila awe mwaminifu na mtu anayefanya majukumu aliyoambiwa. Anatupa tahadhari siku za mwisho watu watakuwa wanasikiliza roho zinazodanganya. Watakuwa wanafiki, wasemaji wa uongo, wakizuia watu wasioe na mafundisho ya vyakula ambayo hayasaidii afya bali ni mapokeo yao tu. Anamwambia Timotheo ajizoeze kwa maneno ya imani, na mafundisho mazuri, bali hekaya za mapokeo ya wazee zisizokuwa na dini azikatae. Watu wengine wamesema kama wao sio mashemasi, je, wanaweza kunywa pombe? La! Kila mtu anaweza kuwa shemasi wakati wowote, na hata hivyo Maandiko yanatukataza mahali pengi tusinywe pombe. Mifano kama ya Nuhu na mingine ni tahadhari tosha kwetu sisi tunaoishi ziku za mwisho.

Timotheo anaambiwa na baba yake wa kiroho mtume Paulo "mtu asiudharau ujana wako, bali uwe kilelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo." Anamwambia afundishe watu, akaripie na kukemea. Ajitunze nafsi yake na Mafundisho ya Kweli. Asimkemee mzee japo ni mshiriki chini yake, bali amwonye kama baba, vijana awaonye kama ndugu na wanawake wazee awape maonyo kama mama zake, na katika usafi wote. Wajane walio na watoto na wajukuu wajifunze kutenda yaliyo wajibu wao. Awaheshimu wajane. Waumini watunze familia zao kwa mahitaji muhimu kama vile chakula, mavazi na malazi. Anakazia akisema, yule asiyetunza wa nyumbani mwake ni mbaya kuliko mtu asiyeamini. Ukarimu unaanzia nyumbani, ila haushii hapo (charity begins at home, but it does not end there).

Anasisitiza kuwa mjane wa kusaidiwa ni yule mhitaji wa zaidi ya miaka 60, na aliyeshuhudiwa mema kwa kuwakaribisha wageni, kuosha watakatifu miguu, na kusaidia wateswao. Wajane wavivu wanaozunguka zunguka tu kwa umbeya na kudoea vyakula vya watu wafundishwe kujitegemea. Muumini akiwa na wajane au wenye mahitaji awasaidie, ili wasiwe mzigo kwa kanisa. Wale wanaolitumikia kanisa kama wachungaji, wasaidiwe mahitaji yao, maana hata ng'ombe anayekokota jembe anakula mazao anayolima na huwa hafungwi mdomo, bali anaachiwa ale yale mazao anayopura. Ila asiwe mwonevu kwa washiriki pale mahitaji yake yamekidhiwa, asilazimishe wamfanyie vitu ambavyo washiriki hao wana uwezo mdogo kufanya. Mfano mwinjilisti anayeenda kuhubiri na kutoa masharti kwa washiriki kwamba "mimi nitakapokuja kwenu nataka muwe mmenunua chakula

hiki au kile, mimi sili chakula cha mbuzi, inabidi mnininulie viatu vipya, na simu mpya n.k). Pia hatakiwa kuwa mbaradhifu, na anayekopa watu pesa naye asilipe. Paulo anasisitiza kuwa mtu akileta mashitaka atafute mashahidi ili ithibitike kuwa ni mambo ya kweli, pia asitoe hukumu kwa haraka. Asimwekee mtu mkono wa uchungaji haraka, na ajilinde na nafsi yake ili awe safi, asije akaangushwa na Shetani. Japo ni mchungaji, ana majaribu yake tofauti, na magumu zaidi hivyo awe makini, maana akijisahau tu ataanguka kwa kishindo. Anamshauri Timotheo anywe maji ya mizabibu kwa afya ya tumbo lake. Neno mvinyo halitenganishi uliochacha na usiochacha kwenye Maandiko kwa lugha yetu ya kiswahili. Damu ya Yesu imefananishwa na mvinyo, usiochacha na siyo matunda yaliyooza.

Anadokeza pia kuwa, waajiri wawathamini waliowaajiri, wasijivune na wamtumainie Mungu. Jambo hili ni zito hasa kwa wale wanaowatendea hiana na ubaya wale wanaowafanyia kazi. Wengine huajiri watoto wadogo wanaofanya kazi masaa mengi, bila kuwasaidia hali wao wanastarehe na watoto wao. Hawampi mtumishi huyu mshahara au hata muda wa kwenda ibadani. Hii ni dhambi, kwani mtendakazi aweza kuanza kazi kutoka saa 11 asubuhi mpaka saa 5 usiku. Waajiri watumie utajiri wao kwa furaha, na kuwa tayari kutoa mali zao kwa wenye mahitaji na kwa kazi ya Mungu. Hii ndiyo akiba ya milele kwao, maana fedha huyeyuka. Siku ya Sabato kazi zifanywe kwa kushirikiana, yaani wote walio katika nyumba hiyo na si mfanyakazi.

Anamwambia ajiepushe na wazimu wa maswali na mabishano ya mijadala ambayo pengine aweza kushinda bali apoteze roho za wengi na kukwaza watu. Ajiepushe na kupenda pesa, maana pesa ni shina la uovu wa yote, akijua kwamba binadamu tumekuja duniani bila kitu na tutaenda bila kitu. Watu wengi wameacha imani kwa ajili ya pesa, na kujichoma kwa maumivu mengi. Anamhimiza akimbie tamaa hiyo aifuate haki, upendo, saburi, upole na utauwa. Ajiepushe na maneno yasiyo ya dini, au maneno yenye elimu ya uongo.

*Wakati Yerusalemu ilikuwa imenyamaza tuli kwa ukimya, na wanafunzi walikuwa wamerudi nyumbani kwao ili kupata burudisho katika usingizi ili kuweza kufanywa upya asubuhi, Yesu hakulala. Maombi yake ya kiungu yalikuwa yakipanda kwa Baba Yake kwa ajili ya wanafunzi Wake, ili waweze kuepukana na ushawishi mbaya ambao wangekutana nao kila siku katika dunia, na ili nafsi Yake Mwenyewe iweze kuimarishwa na kutayarishwa kwa ajili ya kazi na majaribu ya siku inayokuja.
*Kama mwanadamu aliomba kiti cha enzi cha MUNGU hadi ubinadamu Wake ulipoongezewa nguvu (ulichajiwa) na mkondo wa umeme wa mbinguni ambao unapaswa kuunganisha ubinadamu na uungu. Akipokea uzima kutoka kwa MUNGU, Aliwapa wanadamu uzima/uhai.
--------------------------

Maswali: Kwa nini Paulo alimwandikia Timotheo? Mchungaji awe na tabia gani? Shemasi awe na tabia gani? Siku za mwisho watu watakuwa na mafundisho gani ya uongo? Mzee akikosea afanyejwe? Kijana akikosea afanyeje? Wawezaje kumwelewesha mtu mambo ya Mungu bila kubishana naye? Kwa nini Paulo alitaka Timotheo awe mfano bora japo alikuwa kijana?

**SIKU YA 338.**
**(Desemba 3)**

**Waraka Timotheo wa pili.**

# Nimevipiga vita vizuri, Mwendo nimeumaliza, Taji inaningojea.



Paulo aliandika Waraka huu alipowekwa gerezani kwa mara ya pili Rumi. Japo Paulo alitolewa kifungo na Nero kwa muda wa miaka michache akasafiri kuendeleza injili bali alirudishwa kifungoni tena na kuuwawa chini ya Kaisaria Nero (Maandishi ya Historia). Nero alikuwa mtu mkatili ambaye wanahistoria waliandika kwamba alimwua mamaye, mkewe na kisha kakaye kwa sumu ili apate utawala. Paulo anamtia moyo Timoteo kuwa askari wa Kristo aliye shujaa, anayeshika imani na kufundisha ile Kweli ya Neno la Mungu kwa uaminifu. Paulo anatoa wosia kwa mtenda kazi wa huduma ya Mungu. Anamwambia Timotheo asione woga kwa sababu yeye ni mdogo kulinganisha washiriki wengine. Huenda alichunga washiriki wazee na hivyo Paulo anamwambia hao wazee wasiwe tishio kwake, kama wanahitaji kuelekezwa awaelekeze.

Yesu na injili ndiyo nambari moja na si kuogopa washiriki ambao wanaomburuza mchungaji na washiriki wenzao. MUNGU KWANZA ndiyo Kaulimbiu kwetu wanadamu! Anamwomba Timotheo amletee koti lake na Gombo lake kwani ilikuwa

wakati wa baridi. Paulo alikuwa na ukiwa wa kukaa gerezani maana hakuruhusiwa kuwa huru kama wakati alivyoandika kwa Timotheo barua ya kwanza. Hii ndiyo ilikuwa barua yake ya mwisho kabla ya kuuwawa kwa ajili ya imani yake. Marafiki hawakujua pale alipoweka (1:17). Alijua kazi yake ilikuwa karibu imalizike. Wafuasi wengine walikuwa wamemkimbia kama vile Dema, Hermogene, na Figelo. Iskanda mfua chuma alipinga Maneno ya Mungu Paulo anamtahadharisha Timotheo ajiepushe na watu wa namna hiyo. Ila "Onesiforo hakuona aibu na pingu alizowekewa", alimtembelea Paulo na kumburudisha, kwa kumhudumia katika kifungo chake. Hata leo tusiwasahau waliofungwa.

Tito na Tikiko walikuwa wamesafiri, naye alibaki na Tabibu Luka peke yake. Paulo alimpenda Timotheo kama mwana wake, na mtenda kazi bora, kuliko wengi katika kazi ya kumtumikia Mungu. Alihuzunika kwa makanisa yaliyokuwa yanapitia mateso, chini ya Mtawala Nero aliyekuwa mkatili. Amwambia Timotheo ailinde imani, na injili na kuendelea kuihubiri hata kama atapata mateso. Anamkumbuka Timotheo mwana wake na kumwombea usiku na mchana ili aendelee kuichochea karama aliyopewa alipowekewa mikono. Mungu hakutoa roho ya woga kwetu hata leo, bali ya nguvu, upendo na moyo wa kiasi.

Paulo hakuwa na wakili kwenye kujitetea ila Mungu alimsaidia akajitetea na kumwinua Yesu kwa ushujaa, hata wale watu wa mamlaka wakashangaa, ndio sababu walimwachia kwa muda. Ila watu wa mamlaka japo Roho aliwagusa, kama Pilato walitaka kupendeza watu ili wautunze wadhifa wao. Je, wewe leo unatunza wadhifa au hadhi gani? Anamwambia Timotheo, kuhusu Neema ya Mungu ambayo Kristo anatupa. Anasema amepatika na mateso ila hakutahayari kwa vile anamjua Mungu anayemwamini na kuwa anaweza kukilinda kile alichowekewa amana. Anasema nia lazima ikazwe, hakuna anayepigana vita na kujitia katika shughuli za dunia, hata kwenye kushindana kwa michezo bidii yabidi iwepo. Mkulima ili apate mazao anapata tabu ya kazi nyingi, naye pia katika kufungwa imefanya injili ya Mungu iende, maana Neno la Mungu halifungiwi bali linaendelea. Tukipata shida tunapata pamoja na Yesu, tukistahimili pamoja Naye.

Anawaonya washiriki kujiepusha na mashindano ya maneno, na wajitahidi kuonyesha kuwa wamekubaliwa na Mungu, watenda kazi wasiotahayari, wakitumia Neno la Kweli bila kulipindua pindua wanavyotaka. Wengine kama Himenayo na Fileto walileta mafundisho ya uongo kwamba kiyama kimekwisha kuwapo. Anamwonya Timotheo azikimbie tamaa za ujanani, na kufuata haki na amani, upendo. Ajaribu kuepuka ugomvi, maana mtenda kazi wa BWANA hafai kuwa na sifa hiyo ya malumbano. Anatoa tahadhari kwetu siku zetu hizi za mwisho kwamba watakuwa na dhambi za wazi wazi bila kuwa na soni usoni, "Watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiopenda wa kwao, wasiotaka kusuluhishwa, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko Mungu, wenye mfano wa utauwa lakini wakikana nguvu Zake, hao tujiepushe nao.

Watu hawa wanajiingiza majumbani mwa watu na kuchukua mateka mawazo ya watu. Watu hao ni wajinga na wana mizigo ya dhambi. Daima watu hawa watakuwa wakijifunza ila wasiweze kabisa kufikia ujuzi wa elimu ya ile Kweli. Kama wale wachawi wa Farao Yane na Yambre, walivyompinga Musa ndiyo watu hawa wanavyopigana na Mungu, Ila hawatasonga mbele." Je umeshakutana na watu kama hawa? Hebu Bwana atuepushe tusiwe watu wenye tabia hizi ovu! Anamwambia Timotheo yeye afuate mafundisho ya imani kwa uvumilivu, upendo, na saburi kule Efeso. Yeyote amfuataye Mungu ataudhiwa. Anamsifu Timotheo kwa kuwa toka utoto ameyajua Maandiko Matakatifu ambayo yamemhekimisha apate wokovu, kwani "Kila Andiko la Mungu, lafaa kwa Mafundisho, na kwa kuwaonya watu kwa kuwaongoza watu makosa yao, na kuwaadabisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, aliyekamilika apate kutenda kila tendo jema.

Akamwambia awe tayari kwa wakati unaofaa na usiofaa, na kuwa mvumilivu, maana itafika wakati watu watayakataa mafundisho ya uzima na walimu wa hadithi za uongo watatokezea ajiepushe na hao. Kuwa na kiasi, na uvumilivu ni muhimu akifanya kazi yake kama mchungaji. Anamwondoa hofu kwa kumwambia yeye yupo tayari kabisa, kwani "Amevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo ameumaliza, imani ameilinda, baada ya hapo amewekewa taji na BWANA mhukumu wa haki ambayo atampa siku hiyo ya hukumu na wala si yeye tu, bali watu wote wanaopenda kufunuliwa Kwake."

*Maisha ya Maombi ya Yesu Yanafichua Siri ya Nguvu za Kiroho—Maisha ya Mwokozi duniani yalikuwa maisha ya ushirika na asilia (uumbaji) na MUNGU. Katika ushirika huu alitufunulia siri ya maisha ya nguvu za kiroho.


--------------------------

Maswali: Taja tabia za watu wa siku za mwisho. Je, una tabia fulani za watu wa siku za mwisho? Wawezaje kuondokana na tabia hizi? Andiko la Pumzi ya Mungu ni nini? Kila Andiko la Mungu lafaa kwa nini? Wakina nani walimtukimia Paulo katika vifungo vyake? Wawezaje kuvipiga vita vizuri na kulinda imani leo kama Paulo? Kwa nini mtu asikudharau kwa sababu wewe ni mtoto?

**SIKU YA 339.**
**(Desemba 4)**

**Waraka kwa Tito.**

# Tabia ya Mchungaji, tabia ya mzee wa kanisa.



Waraka wa Tito umeandikiwa Tito mzee wa kanisa au mchungaji kijana ambaye alikuwa mwongofu ambaye Paulo alimsaidia kumleta kwa Yesu Kristo. Wadhifa huu na ule wa Timotheo unashabihiana sana. Hakika mausia haya ni ya kila muumini au mshiriki leo. Paulo alipoenda Yerusalemu kujadili Injili kwa mataifa na viongozi Yerusalemu alimchukua Tito mtu wa mataifa, ila wa imani Ya Kristo. Tito alikuwa mtenda kazi mwenzake na Paulo, ila hakutahiriwa kama Timotheo au Wayahudi. Paulo alimtuma Tito Korintho pia kutatua matatizo. Tito alifanya kazi na Paulo tena, baada ya Pulo kupata nafuu kidogo ya kifungo Rumi. Tito alifanya kazi pia Dalmatia ambayo ni Yugoslavia ya zamani, au Serbia. Tito alionekana kuwa na maadili na uaminifu katika utendaji wa kazi.

Paulo alihubiri kisiwa cha Krete, na akamwekea mwanafunzi wa Kristo na mwenzi wake Tito mikono, achunge kundi lile, kisha aliondoka. Aliandika barua hii akiwa Korintho au Nikopolisi. Paulo anasema alimwacha Tito Krete ili ayatengeneze yaliyopunguka, na kuwawekea wazee mikono kama viongozi wa kiroho katika kila mji. Wengine walikuja na mafundisho ya kuwachanganya waumini kwa kusema lazima washike sheria za mafarisayo. Anaandika tabia na wasifu wa kuangalia katika kuchagua viongozi wa kanisa. Mzee wa kanisa aweze kuwa mtu anayeamini, asiyeshtakiwa kuwa mfisadi au mwenye mawaa, au asiyetii. Wakrete walikuwa wana maadili yaliporomoka na kumomonyoka, hata nabii wao na mtunga mashairi alisema Wakrete ni waongo siku zote, watu wakatili kama wanyama, walafi na wavivu 1:12. Paulo anasema ameiona tabia hii, ni kweli ndivyo ilivyo.

Paulo anampa mamlaka toka kwa Mungu, awakemee kwa ukali, ili wapate kuponywa imani yao ili wasiangamie. Tena anasisitiza pia, wasisikilize hadithi za Kiyahudi, maana hao wanamkiri wanamjua Mungu, bali kwa matendo yao, wanamkana. Hao ni wenye machukizo na waasi. Askofu au mchungaji, na hata viongozi wote wa kiroho wasiwe watu wa kushitakiwa neno baya, maana wanamwakilisha Mungu. Anaorodhesha, Wasiwe watu wa tabia hizi mbovu: kupendeza nafsi, mwenye kukasirika haraka, walevi, wagomvi au wapenda mapato ya aibu. Askofu anatakiwa

awe mkaribishaji na mkarimu kwa watu, mpenda mema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake, akilishika Neno la imani, vile vile kama alivyofundishwa, apate kuwaonya wengine kwa Mafundisho yenye uzima na kuwashinda wenye kuyapinga Maneno ya uzima.

Wazee wa makanisa vivyo hivyo wawe wenye kiasi, wastahivu, wenye busara, wazima katika imani na katika upendo na katika saburi. Wazee wa kike pia nao wawe na mwenendo wa utakatifu, wasiwe wasingiziaji, wasengenyaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo, bali wafundishao mema, ili wawatie wanawake ambao ni vijana akili za kujua kutunza miji yao kwa kuwapenda waume zao na watoto wao, wakiwahudumia na kuwasaidia kama wakina mama nyumbani. Wanawake hawa walioolewa ambao si wazee, wawe na kiasi, safi katika mawazo, maneno na matendo, wawatii waume zao, maana wasipofanya hivyo watu watalitukana Neno la Mungu. Maana hata watu wa mataifa wanaheshimu waume zao, maana ni amri toka kwa Mungu.

Vijana wa kiume waonyweshwe kielelezo cha matendo mema, na katika kujikana nafsi, mafundisho ya ustahivu, na maneno ya uzima, na tabia njema ili hata yule mwenye kumpinga Kristo aweze kuaibika maana hana baya la kusema kuhusu watu wa Mungu. Watumwa au waajiriwa wafundishwe kutii bwana zao, wakiwapendeza katika mambo yote, wasiwe wenye kujibishana ovyo, au wezi, bali waonyeshe uaminifu mwema kwa wote, ili wayafanye Mafundisho ya Yesu Mwokozi kuvutia watu, maana Neema ya Mungu ituokoayo wanadamu wote imefunuliwa nayo yatufundisha wote Wakristo na waumini, kukataa ubaya na tamaa za dunia, tukiishi kwa kiasi, haki na utauwa katika ulimwengu huu wa sasa. Maana tunatazamia tumaini lenye baraka yaani Kurudi Kwake Yesu Kristo Mungu Mkuu na Mwokozi wetu atuchukue.

Ni muhimu kutii mamlaka zilizowekwa kutuongoza katika nchi, na kila Mkristo ajifunze kutotukana, kutokuwa mgomvi, bali wawe mwema na mpole, kwa watu wote. Maana tabia mbovu tulizifanya kabla hatujamjua Kristo, tukaishi kwa kuchukiana, wivu, anasa, bali kwa rehema Yake ametuosha na tumezaliwa upya mara ya pili, na kufanywa na Roho Wake Mtakatifu. Tujiepushe na maswali ya upuuzi na magomvi ya mashindano, hayana faida wala maana, tuepuke uzushi. Tito 3:3-8 ni muhtasari wa injili yote!

Paulo anasisitiza tuache uovu na kuishi maisha ya utauwa. Kwa nini? kwasababu Neema ya Yesu imefunguliwa kwetu sote, nayo yatufundisha kukataa tamaa za dunia na uovu wote, ili tuishi maisha ya kiasi na utauwa, tukitazamia tumaini la baraka yaani kuja kwa Yesu mara ya pili. Tukumbuke tabia anazopaswa kuwa nazo mchungaji ni tabia hizo hizo anazopaswa kuwa nazo kila muumini, au yoyote ampendaye Mungu! Hii ni kwa sababu sheria za Mungu ni zile zile kwa binadamu wote. Hakika neema ya Mungu imefunguliwa kwetu! Kikubwa kwetu ni "Tulinde moyo wetu kuliko yote tuyalindayo; Maana ndiko zitokako chemchemi za uzima." Moyo wa mwanadamu ambao haujaongoka ni kitu cha kuogopesha. Matendo mazuri ya upendo na wema hutokea duniani kila dakika ya siku husika, lakini hakuna shaka kwamba uovu umetawala vivyo hivyo kila mahali tunapotazama. Tunapokumbana na vita zisizokoma, ufisadi wa kisiasa, na ugomvi kwa kiwango kikubwa, tunapaswa

pia kukubali kwamba wakati wowote matendo ya uonevu yanapotendwa, mioyo ya kibinadamu iliyovurugwa ipo kazini. Kwa kweli, Biblia haina mema mengi ya kusema kuhusu mioyo ya wanadamu ambayo haijasalimishwa kwa Yesu Kristo. Mungu anasema, "Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua?" (Yeremia 17:9). Moyo ambao Mungu anauzungumzia hapa si "mashine inayosukuma damu" iliyoko ndani ya vifua vyetu bali ni "moyo wa akili" zetu na makao ya kufikiri kwetu, kiini cha ufahamu wetu na maadili, kijito ambacho kwacho shauku hutiririka. Yesu aliweka wazi zaidi alipotafakari kuwa, "Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa yaliyo maovu; kwa kuwa mtu, kinywa chake hunena yale yaujazayo moyo wake" (Luka 6:45). Matendo yetu yote, mema au mabaya, chanzo chake ni katika akili. Ni akili ndiyo inayomwabudu Mungu na kutuunganisha na viumbe wa kimbingu" (Mind, Character, and Personality, gombo la 1, uk. 72). Ni akili ndiyo Mungu anayotafuta ili kuisajili katika Pambano dhidi ya ubinafsi na uovu. Ni mbaraka kiasi gani kufahamu kwamba akili zetu zinaweza kutengenezwa upya kwa Neno la Mungu linaloponya! Moyo au Akili zinapaswa kutunzwa, kuhudumiwa, na kulindwa. Tunapaswa kumwomba Mungu atengeneze ndani yetu mioyo na akili safi (Zaburi 51:10), lakini tunapaswa kuilinda zawadi hii kwa umakini wote. Majira ya kawaida ya muda binafsi unaotumiwa katika sifa, maombi, kujifunza Biblia, na kushuhudia yatafanya mengi zaidi katika kulinda akili zetu ndani ya Kristo Yesu kuliko kitu chochote tunachoweza kufanya kila siku: "Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini" (Isaya 26:3). Tunza akili yako, hata wakati ambapo kila mmoja anapoteza ya kwake!

*Yesu Aliomba Katika Kujitayarisha kwa ajili ya Kazi maalum—Yesu, alipokuwa akijitayarisha kwa ajili ya jaribu kubwa au kazi fulani muhimu, aliondoka na kujitenga katika milima yenye utulivu na kulala usiku kucha katika sala kwa Baba Yake. Usiku wa maombi ulitangulia kuwekwa mikono/wakfu kwa mitume na Mahubiri ya Mlimani, kugeuka sura kwa mng'ao, uchungu wa jumba la hukumu, msalaba, na utukufu wa ufufuo. Sisi pia lazima tutenge nyakati kwa ajili ya kutafakari na kusali na kupokea burudisho la kiroho. Hatuthamini nguvu na ufanisi wa maombi jinsi tunavyopaswa.

--------------------------

Maswali: Kwa nini watumwa au waajiriwa watii mabwana zao? Kwa nini ni muhimu Mkrito asiwe mtu mtukanaji na mgomvi? Tumaini la baraka ni nini? Mzee wa kanisa, askofu, na wazee wa kike wanapaswa kuwa na tabia gani? Kwa nini ni vyema tusifanye watu wadharau utoto au ujana wetu? Je maisha yako yanaendana na Tito 2:7,8, Kwanini tulinde mioyo na akili zetu?

**SIKU YA 340.**
**(Desemba 5)**

**Waraka kwa Filemoni.**

# Msamehe Onesimo na mchukue kama Ndugu



Paulo aliandika barua hii pamoja na ile ya Wakolosai wakati mmoja, kwa kuangalia utangulizi wake, alikuwa na Onesimo na Tikiko, akiandika barua hizo mbili gerezani Rumi. Paulo alimwandikia Filemoni, muumini wa mji wa Kolosai, aliyempenda Yesu na kuwa mkarimu kwa wageni. Filemoni alikuwa na watumwa, zama zile za giza jambo hili ambalo si jema lilikuwa la kawaida. Mmoja wapo wa watumwa wake Onesimo, alikuwa amemwibia na kutoroka. Kwa sheria za Rumi jambo kama hili lilikuwa adhabu ya kifo.

Mtumwa siku hizo alikuwa mali ya bwana wake, na alikuwa na mamlaka makuu kwa huyo. Karibu Warumi wengi walikuwa na watumwa kuwasaidia kazi za nyumbani, shambani na biashara. Mtumwa hakupata mshahara bali chakula, nguo na mahali pa kulaza kichwa chake. Onesimo aliishi maisha ya kujificha-ficha akiogopa asigundulike. Ila Onesimu alikutana na Paulo na kutokana na huduma yake, akawa Mkristo Mwongofu. Onesimo alimhudumia mtume Paulo, ila Paulo aliona ni vizuri kuweka mambo sawa na bwana Filemoni. Hii ingeweza kumsaidia Onesimo asiishi kama alivyoishi zamani.

Paulo alizungumza na Onesimo, na akawa radhi kurudi kwa bwana wake Filemoni. Hapo ndipo Paulo akamwandikia Onesimo barua ya kumwombea radhi, na kumsihi amsamehe na kumpokea kama ndugu yake katika Kristo ili kumfanya awe tayari kumpokea Onesimo. Onesimo pengine alikuwa tayari kurudi ila hakujua aanze vipi. Paulo anaandika kwa hekima na kwa upendo, akitumia maneno ya kumvuvia, ili kumfanya ashawishike kwa lile analojaribu kuandika.

Paulo anasema Yeye ni mfungwa wa Kristo Yesu, anaandika akiwa na Timotheo na watenda kazi wengine katika Kristo. Anamshukuru Mungu siku zote, na anamkumbuka Filemoni katika maombi yake, kwani amepata faraja nyingi, kwa kuwa ameburudisha watakatifu wengi. Filemoni alikuwa mtu mwenye mali, na alipoongoka, alisaidia watakatifu wengi waliokuwa na mahitaji na hata wale waliotaka kuhubiri katika Kolosi.

Paulo anasema amepata ujasiri wa kumwandikia kwa ajili ya tabia yake huyu bosi, yenye upendo kwa ndugu na ukarimu, anaowafanyia watakatifu na watu wote. Paulo ambaye ni mzee kwa Filemoni, anamwandikia huyu ndugu katika Kristo kwa hekima kuu, kama mtoto wake katika imani, akimsihi kwa ajili ya Onesimo, aliyemzaa kiimani katika vifungo vyake Rumi. Anamwambia Filemoni, kwamba zamani Onesimo alikuwa si mtu mwaminifu wala wa kumfaa, ila sasa atamfaa, kwani hata sasa kule Rumi ni msaada sana kwa Paulo. Paulo angeweza kuamrisha, lakini anaandika kwa upendo na hekima.

Paulo amsifia Onesimu ni ‘moyo wake hasa’. Anasema kwa upendo wake angetaka Onesimo akae naye, ila kwa kisheria, ni mali yake Filemoni, kwani ni mtumwa aliyetoroka hivyo anamwomba ruhusa na mashauri kama ikiwa ni vyema kwake, na si kwa kushurutisha ampokee tena Onesimo, ambaye walitengwa naye kwa muda baada ya wizi. Lakini kwa vile amempokea Kristo, na amekuwa sasa ndugu katika BWANA, na si mtumwa tena. Paulo anamsihi, kwamba ikiwa Onesimo anamthamini Paulo kama ndugu na baba katika imani, basi ampokee Onesimo kwa niaba yake. Paulo ameandika barua kwa mkono wake mwenyewe, anamwomba Filemoni, akisema ukinifanyia hivi utaburudisha moyo wangu.

Anamaliza kwamba ameandika haya kwa vile anajua Filemoni ni mtauwa anayependa kutii, na anajua kwamba atamfanyia Onesimo, mema zaidi ya kumpokea tu au zaidi ya yale Paulo anamsihi amfanyie. Barua hii hata leo inatuhusu, wale ambao wako katika nafasi kuwa na ukarimu na huruma kwa watenda kazi wao. Tabia hii ya Kristo, ya kuwaombea watu msamaha na kusimama kama mpatanishi pale mtu amekosa ili kuleta mahusiano au upatanisho ni muhimu. Waajiri, viongozi wa siasa, wazazi hata wale wenye nafasi muhimu mahali fulani; tufuate mfano wa Paulo, wa kuwatendea mema watu wa imani, kama watenda kazi wenzetu na viungo vya mwili wa kanisa. Mathayo tano inasema waheri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu.

Hatupati jibu la Filemoni bali tunaweza kusema, aliyafuata maneno ya Paulo na kumchukua Onesimo tena. Si kama mtumwa tu bali kama ndugu katika BWANA; maana mtumwa siku zile alikuwa ni mali ya bwana wake, hakupata mshahara,

na akapata mateso mengi kama bwana alikuwa ni mkatili. Hebu wale wenye watenda kazi wawe na huruma na kuyatetea maslahi yao, wakitendea kama vile wao wangetaka kutendewa. Mtu asifanye kazi bila malipo, au bila kuendelezwa kwa elimu kwa namna fulani, na ukifika wakati wa kuoa au kuwa na mahali pake, hebu basi na asaidiwe, asiachwe aende mkono mtupu. Na Siku ya ibada ya Sabato wawasaidie kazi zote za wanazofanya ndani, au wawaache wapumzike, na wale wafanyikazi, waepuke uovu wa kuwaibia matajiri wao, au kuwafanyia hiana kwa kuwagombanisha na watoto wao, au na waume/wake zao. Mwajiri awe mtu wa kumheshimu na kumpenda mtumishi wake.

mtenda kazi asiwe mtu anayekosa utii kwa mamlaka au mvivu asiyefanya kazi anayoambiwa. Watenda kazi wengine wamekuwa wezi na kufanya mambo ambayo si mema kwa familia wanayoifanyia kazi, wakisimulia visa kwa mwajiri vya uongo, au umbeya, nao wakitaka watu wamchukie yule mwajiri. Kila kitu kitaletwa hukumuni.

*Ikiwa Mwokozi wa wanadamu, pamoja na nguvu Zake za Uungu, alihisi hitaji la maombi, ni zaidi kiasi gani basi kwa wanadamu wanyonge, wenye dhambi wanaokufa wanapaswa kuhisi ulazima wa maombi—Sala ya bidii na ya daima! Wakati Kristo alipozingirwa na majaribu makali zaidi, Hakula chochote. Alijikabidhi kwa MUNGU na, kupitia maombi ya dhati na utii mkamilifu kwa mapenzi ya Baba Yake, aliibuka mshindi. Wale wanaoshuhudia ile Kweli katika siku hizi za mwisho, juu ya kila tabaka jingine la wanaodai kuwa Wakristo, wanapaswa kumwiga Yule ambaye ni Kielelezo Kikuu katika maombi.
-----------------------------

Maswali: Kwa nini Paulo aliandika barua hii? Kwa nini Paulo angetaka Onesimo akae naye? Filemoni aliishi wapi? Barua hii inatuhusuje leo sisi? Je, waweza kubuni kilichotokea baada ya barua hii kwa Filemoni na Onesimo? Kwa nini kumfanya mtu mtumwa ni dhambi? Yasemekana siku hizi kuna watumwa wengi zaidi ya zamani, watoto na watu wazima, Je, wawezaje kusaidia watu wa namna hii waliouzwa ili kutumikia watu katika ulimwengu wa leo yaani 'human traffiking' hapa afrika na hata nchi zingine kama Uarabuni?

Kwa maneno mengine ya leo -Soma hii barua
Filemoni, rafiki yangu mpendwa—

Ningeweza kukubamiza kwa kukuamrisha na ukuu wangu na kukulazimisha ufanye ninachotaka—mimi, hata hivyo, mimi mtume Paulo, niliyeandika kutoka gerezani kwa ajili ya Injili. (Kumbuka, una deni kwangu wewe mwenyewe sana!—lakini sitaisugua hiyo ndani.) Kwa hivyo badala ya kukulazimisha kwa hali au kwa mamlaka yangu, ninauvutia moyo wako. Upendo wako ni maarufu sana na umekuwa kitia-moyo sana kwangu—na ninakujua vyema—nina hakika utanifanyia upendeleo huu.

Amini usiamini, nimekuwa baba hapa gerezani! Mwanangu ni Onesimo wako mwenyewe, ambaye hapo awali hakuwa na faida kwako, kama jina lake linavyoonyesha, lakini sasa ananifaa sana. Kwa kweli, sipendi kumrudisha kwako,

yeye ni msaada sana, na nimekuja kumpenda kama wangu. Hata inaonekana anachukua nafasi yako katika kurahisisha maisha yangu hapa gerezani, jambo ambalo najua ungefanya kama ungekuwa hapa.

Lakini Onesimo yuko pamoja nawe, si kama mtumwa, bali sasa ni ndugu katika Kristo. Tafadhali mkaribishe tena kama alivyo. Mfungulie moyo wako kama vile ambavyo ungenipenda mimi, kwa sababu kama mwanangu katika Injili, Onesimo ni sehemu yangu mimimwenyewe!

Natumaini kukutembelea hivi karibuni.

Wako katika imani,
Paulo

**SIKU YA 341.**
**(Desemba 6)**

**Waraka kwa Waebrania.**

# Yesu ni bora kupita vyote. Kafara Yake, ni bora, Ukuhani Wake ni Bora..........



Waebrania ni wazao wa Ibrahimu kupitia kwa Isaka. Agano la Kale liliandikwa kiebrania. Barua hii ndefu kupita zote za Paulo iliandikwa kwa waumini ambao ni Waebrania kwa asili, basi hata kwetu leo ina mafundisho mengi. Yesu, mitume na Wakristo wa kwanza walikuwa Waebrania. Walikuwa kwenye utamaduni wa dini ya kiyahudi, wakienda kwenye hekalu na kuomba, na kutoa kafara. Mfumo wote wa kutoa kafara kama kielelezo cha wokovu ilibidi ueleweke kwa kila mmoja wao. Mfumo huu Mungu aliuweka ili kututoa kwenye makucha ya Shetani.

Yesu alikuja na kufa, kwa dhambi zetu ili hatia hii itoke. Ilikuwa vigumu kwa wale waliokuwa katika uyahudi, walipoongoka kuwa Wakristo. Ndipo walipoacha mapokeo ya kafara, na mengineyo baada ya Yesu kufa. Barua hii yaeleza utume au kusudi la Yesu Masihi na kutuambia kwa wazi kazi ya Yesu sasa. Wengi wanasema barua hii ni ya Paulo kutokana lugha au mtindo wa kuandikwa kwake; ila haijulikani kwa wazi. Barua hii iliandikwa kuelezea mwisho wa kafara za Agano la Kale baada ya hekalu kubomolewa na Jemedari Tito mwaka 70 A.D. Pazia nene la hekalu lilipasuka kutoka juu hadi chini baada ya Yesu kufa, na hata kondoo aliyekuwa anaenda kuchinjwa alikimbia! Dhabihu kuu, ile halisi ya Yesu ilikuwa imetolewa, nayo ilitosha kabisa.

Mungu zamani alisema na baba zetu kupitia manabii na njia zingine, ila sasa anasema kwetu kupitia Mwana wake Yesu Kristo. Hili tunapasa kulitilia makini, maana hata yale waliyonena malaika yalikuwa ya muhimu. Je, haya ambayo ni ya Yesu Mwana wa Mungu "Tutapataje kupona tusipoyajali?" Uchumi wa Wayahudi ulikita sana kwenye wanyama wa kafara, watu walijipatia pesa wakiuza mifugo. Hata hekalu

lilipata kodi; wakasahau kabisa kwamba ile kafara ya kuchinja wanyama ni mfano tu au kivuli cha ile kafara halisi ya Yesu atakayekuja kuitoa kwa kufa msalabani.
Waebrania inakazania ubora na ukuu wa Kristo, kama kafara isiyo na mawaa ya Kuhani wetu mkuu na halisi, wa kweli na Bora kupita wote. Yeye hana haja kama makuhani wengine kutoa kafara kwanza kwa dhambi Zake kisha zetu, maana Yesu hakuwa na dhambi, hivyo, Yeye alijitoa mara moja tu kwetu. Ukuhani wa Walawi au wachungaji wa uzao wa Haruni na binadamu wote una mapungufu mengi. Kristo ni mkamilifu na Mtakatifu, ni kafara Yake tu ambayo inaweza kutuondolea makosa yetu. Ilimpasa Yesu kufananishwa nasi kama ndugu Zake katika mambo yote ili aweze kuwa kuhani Mwenye rehema na mwaminifu katika mambo ya Mungu, na kufanya suluhu ya kutupatanisha na dhambi zetu.

Basi leo tukisikia sauti Yake tusifanye mioyo yetu kuwa migumu kama wana wa Israeli ambao walitangatanga jangwani miaka 40. Soma Walawi 16 na Kutoka 25 na inahusiana sana na kitabu hiki. Walawi na Kutoka kilikuwa ni kivuli, mfano au picha ya kifo cha Yesu ambacho ndiyo kitu halisi kinachoondoa dhambi zetu. Leo tujue tuna kuhani mkuu Yesu aliyeingia mbinguni, anayechukuliana na udhaifu wetu. Yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote ila hakufanya dhambi. Tukaribie Kwake kwa neema na ujasiri ili tupewe rehema ya kutusaidia. Yesu ni bora kuliko malaika, au kafara zote. Hebu kila mmoja wetu kwa imani aangalie mbinguni na pale kwenye hekalu amwone Yesu mahali Patakatifu pa Patakatifu akituombea na kututetea.
Zamani watu walikuwa na miungu ya miti na mawe, ila siku hizi watu wana miungu ya vitu kama vifaa vya teknologia mfano simu, runinga, Kompyuta, chakula, watoto, maoni, urembo, tumbo, mavazi, magari, nyumba na vitu vingine. Je wewe una miungu gani? Ni mmoja tu anastahili kuwa namba moja katika maisha yetu. Mungu na Mwana Wake Yesu Kristo. Yesu ana kila kitu bora, ni kuhani bora, Mwenye maagano bora, Mwenye tumaini bora na Kafara bora kupita zote. Mweke Yesu katika sehemu zote za maisha yako, na kila kitu kitaenda sawa.

Kitabu cha waebrania kimenukuu Agano la Kale mara kadhaa. Kitabu hiki kinahusiana na kafara, kama vile kitabu cha Walawi kilivyo, katika Agano la Kale. Dhambi iliingia kwa mtu mmoja, na kutolewa na Mtu mmoja Yesu Kristo. Basi imetupasa kuyazingatia haya tunayoambiwa tusije tukakosa ahadi ile ya kuingia katika raha Yake. Tukaze mwendo ili tufikilie utimilifu. Maana Yeye aweza kabisa kutuokoa sote tumjiao Mungu, kwa maana Yeye Yu hai siku zote, ili atuombee sisi.
Kitabu hiki kinatueleza pia kwamba kama vile wana wa Israeli walivyokuwa na hekalu, au madhabahu kule nyikani, kuna hekalu pia mbinguni lililo na Patakatifu pa Patakatifu ( Waebrania 9 na Kutoka 25). Hili ndilo hekalu halisi (original and real), lile la madhabahu ya kukutania la 'Musa' lilikuwa ni mfano, au kivuli cha lile la mbinguni. Katika hekalu lile la jangwani la Musa, kila siku kuhani alitoa kafara asubuhi na jioni Kutoka 39:29, na kisha kuhani aliingia mara moja kwa mwaka kuombea dhambi za watu Walawi 16. Ila kuhani wetu Yesu Kristo katika madhabahu ya mbinguni, hatumii damu za wanyama kama ng'ombe au mafahali, bali damu Yake kwa kifo Chake msalabani kwa mara moja tu milele zote.

Kristo hakuingia Patakatifu pa mwanadamu, kutoa kafara bali Patakatifu halisi,

aonekane usoni pa Mungu, Naye ameingia mara moja tu na siyo kila mwaka. Akiisha kutolewa sadaka mara moja amezichukua dhambi za watu wote, na atatokea mara ya pili pasipo dhambi kwa wote tunaomtazamia. Paulo anatupa wosia tusiache kukutanika kila wiki kwenye ushirika, tusikae majumbani mwetu bila kwenda ibada "bali tuonyane Na kukutana kadiri tuonavyo siku ile inakaribia." 10:25. Kitabu hiki ni muhimu kwetu waumini wote, kwani kinatueleza huduma ya Yesu kama kuhani wetu mkuu mbinguni, leo hivi. Yeye ni Mwana wa Mungu na mwanadamu pia. Katika kofia Yake ya Kuhani Mkuu anatupatia njia kumwendea Baba wa mbinguni kwa maombi.

Paulo aliwaandikia Wayahudi kuwa waaminifu maana walikuwa wakiyumba yumba. Wengine walirudi nyuma na kutaka waendelee na kafara zilizopitwa na wakati ambazo zisingesaidia. Hata leo Wayahudi wengi wanaendelea kutoa kafara, wakingojea Masihi. Ila sisi tujue, Yesu ni kafara bora kupita zote, na anaishi leo, akituombea, kama kuhani wetu. Imani ni kuwa na uhakika wa mambo tunayotarajia, japo hatuyaoni. Wazee wa imani, kwa imani walimwamini Mungu, Japo walipata mateso na mitihani, matendo yao yalienda na imani yao. Kuanzia Abeli aliyetoa kafara kwa vile alielewa mpango wa wokovu na vile mwana kondoo anavyomsimamia Yesu, Mwana-Kondoo wa Mungu.

Henoko pia alisikia maagizo na kuishi inavyopasa, Nuhu, Ibrahimu, Sara, Nuhu, Eliya, Danieli, Paulo, Ayubu, Yohana na wengine wengi, wote walisafiri safari hii ya imani. Hawa walitegemea mji ambao Mungu amewatayarishia. Japo hawakuupokea ule mji wa mbingu na nchi mpya mpaka wakalala usingizi wa mauti; walijua watafufuliwa siku moja na kupata ahadi ile ambayo Mungu alikuwa amewaahidia. Kwani Mungu ni Mwaminifu na wa kweli. Ukijiwa na mafikara ya kukata tamaa kwa maisha magumu unayopata, soma Waebrania 11 uone jinsi watu hawa walivyovumilia mateso mengi ya ajabu kwa imani yao, na pia Yesu, ila thawabu yao ni kubwa. Ile orodha ya Waebrania 11 ya imani, inaendelea kuandikwa hadi leo, ni maombi yetu kwamba nasi tumo katika orodha. Nasi tupige mbio kwa saburi na faraja.

Biblia imeandika Neno imani mara 247, na ni mara mbili tu Neno imani limeandikwa kwenye Agano la Kale, ila hapa tunaona imani ya Agano la Kale imeletwa hapa pia! Je, kama siku hizi tungepaswa kutoa kafara, tungeweza? Nafikiri maisha yangekuwa ghali mno. Ila Yesu ametenda yote kwetu! Na Mungu haoni aibu kuitwa Mungu wetu. Basi kwa nini sisi tumwonee aibu mbele ya watu nasi tu wanyonge na tupu? Mwandishi anatuambia ubora na ukuu wa Kristo na kazi Yake kwenye madhabahu kama Kuhani Mkuu. Maandiko yazungumza kuhusu ukuhani wa Walawi, na kusema upungufu wa Agano la Kale na kafara Zake ukilinganisha na ukamilifu na Utakatifu wa Kristo. Tusome Neno la Mungu, kwani li hai tena lina nguvu na ukali kuliko upanga ukatao kuwili. Neno lakata na kugawa roho na viungo. Neno lina wepesi wa kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Kila kitu ki wazi mbele Yake, kwani kimefunuliwa na kuonekana vizuri kabisa. Hebu tumwombe Mungu atusaidie kuithamini kafara hii na kuwa na ujasiri kumwomba msamaha na kuishi kwa kumthamini Yeye.

Sote tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi hivyo tuweke kando mizigo yetu ya dhambi ituzingayo kwa wepesi. Hebu na tupige mbio kwa saburi tukimtazama Yesu Mwenye kuanzisha imani yetu ambaye kwa ajili ya furaha aliyoiona tukiwa Naye mbinguni; aliustahimili msalaba na kuipuuzia aibu, Naye ameketi mkono wa kuume wa Baba mbinguni. Hatujamtetea Mungu hata kumwaga damu, maisha yetu si magumu vile, hebu tuwe tayari kurudiwa na BWANA. Tunyoshe mikono iliyolegea na magoti yaliyopooza. Tukitafuta kwa bidii kuishi kwa amani na utakatifu na watu maana hakuna atakayemwona Mungu bila hayo. Tumfanyie Mungu ibada ya kupendeza.

Tuendeleze upendo wa ndugu, tusiache kuwakarimu wageni, maana wengi wamekaribisha malaika bila kujua. Tukumbuke kuwatembelea walio magerezani. Tusipende fedha bali tumpende Mungu, maana amesema "sitakupungukukia kabisa wala sitakuacha kabisa." Tukumbuke hapa hatuna mji unaodumu, kila kitu kinapita ila tunatumainia mji ujao wa mbinguni. Tunashauriwa kutii watawala wa serikali na walio katika mamlaka, maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zetu, hebu tuwafanye wawe na furaha kutuhudumia na kutumika kwa ajili yetu.

Basi Mchungaji au Kuhani wetu mkuu wa kondoo, ambaye Ndiye Yesu atusaidie tuwe wakamilifu, katika kila tendo Jema, tupate kufanya mapenzi Yake. Upendo wa ajabu kama nini! Kwamba Yeye aliye sawa na Mungu, na mkuu kuliko malaika, hakuona kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho, bali alijifanya kuwa si kitu, akatwaa namna ya mtumwa, akifananishwa na wanadamu, akashika nafasi ya chini, na akamtii Mungu. Mungu hakuacha chochote, iwe ni juhudi au gharama, ili sisi tupate kuokolewa. Ikiwa tunathamini upendo huu wa ajabu, wokovu huu mkuu sana, kwa nini tusiache kila kitu ili kupokea zawadi Yake ya wokovu? Hebu tupokee ujumbe huu na tutoe kafara yale tunayopaswa ili kwamba hakuna kitu chochote kinachoweza kusimama kati yetu na Mwokozi wetu. Bwana tunaomba utusaidie! Utukufu una Wewe milele na milele.

*Yesu Alisali Mapema Asubuhi—Asubuhi na mapema mara nyingi ilimkuta katika sehemu fulani ya faragha, akitafakari, akichunguza Maandiko, au katika sala. Kwa sauti ya uimbaji alikaribisha mwanga wa asubuhi. Kwa nyimbo za shukrani alizishangilia saa zake na kuleta shangwe ya mbinguni kwa wale waliochoka na kazi zao za kila siku na waliovunjika moyo.


---------------------------

Maswali: Kwa nini Yesu ni bora kuliko kafara za wanyama zilizotolewa? Kwa nini ni muhimu kuwa na ukarimu kwa wageni? Kwa nini ni muhimu kwenda kanisani? Kwa nini tutembelee walio magerezani? Kwa nini tuheshimu viongozi wa serikali? Imani ni nini? Je, siku hizi watu wana miungu gani? Kwa nini ukuhani wa wanadamu una mapungufu mengi? Kwa nini ukikata tamaa kwa kuwa na matatizo mengi usome Waebrania 11? Mtu anawezaje kufanya maoni, falsafa au mtazamo wake kuwa Mungu?

**SIKU YA 342.**
**(Desemba 7)**

**Waraka wa Yakobo.**

# Imani bila matendo ya kumpendeza Mungu, imekufa.




Barua hii ni ya Yakobo, ndugu ya BWANA Yesu na mmoja wa mitume 12. Yakobo hakuwa muumini mpaka Yesu alipofufuka na kumtokea. Yakobo alikuwa mkuu wa baraza Yerusalemu Baraza la kwanza la waumini waliomwamini Yesu Kristo. Alijua mengi toka utotoni ya kuishi na BWANA Mwenyewe. Je, umejiuliza yale aliyojua kuhusu Yesu kama kaka yake! Huyu si Yakobo mtume au mwana wa ngurumo au Yakobo mtume wa kwanza kufa kwa kuuawa na Herodi mwaka 44BK. Wakitaja ndugu wa Yesu kwenye Maandiko, huyu Yakobo jina lake latajwa kwanza.

Yesu alimtokea baada ya ufufuo, na Paulo amwita nguzo ya kanisa katika barua zake, kwa ajili ya kazi aliyoshikilia. Paulo alipoongoka alienda kumwona huyu Yerusalemu. Wakati Petro amefunguliwa aliwaaambia marafiki zake wamweleze Yakobo. Yuda aliyeandika waraka na Yakobo ni wana ndugu. Anaandikia makabila 12 ya watu waliotawanyika. Anaandika yahusuyo sheria, maadili ya jumuiya, imani na matendo, kukua kwa imani, na matendo ya tunda la roho. Anasisitiza maneno yetu yaendane na matendo, kuzungumza ni rahisi ila kuenenda katika imani ni mpando. Maneno yetu yafanane na mtindo wa maisha. Siyo habari tu ya kuwa mkristo bali ya kutembea na Kristo. Tukumbuke hata Shetani anaamini na kusadiki Mungu Yupo na anatetemeka. Kristo alipotembea hapa dunia, mashetani yalimkiri na kutetemeka. Hivyo tuwe watendaji wa Neno na sio porojo tu. Anazungumzia

kutenda mema, ila anakazia kuwa mwema.

Yakobo anasema ni furaha tukipata majaribu maana kujaribiwa kunaleta saburi na ukamilifu. Anatushauri tuombe hekima sote, maana Mungu awapaye wote, atatupa ila tukiomba tuamini tumepewa. Tusiwe wenye shaka, au nia mbili tukichukuliwa na upepo huko na kule. Yoyote anayestahimili majaribu atapokea taji ya uzima. Ila mtu akijaribiwa asiseme Mungu ananijaribu, kwani kwa kawaida anajaribiwa na tamaa zake. Mungu hutoa vitu vizuri tu na si vibaya. Mtu akidhani anayo dini ila hazuii ulimi wake, bali huropoka tu, bila kufikiria, anajisumbua kabisa.

Dini ya Kikristo yataka tutawale nafsi na kuwa na kiasi. Ulimi ni kiungo kidogo, ila waweza kuwasha moto kama wa Jehanamu. Wanyama kama farasi, na hata meli zimeendeshwa kwa lijamu na misukani midogo, ndiyo ulivyo ulimi. Asema walimu wana hukumu kubwa maana Mungu amewakabidhi majukumu makubwa, hivyo watumia ndimi kwa hekima ya mbingu. Kamwe watu wazima wasizungumze maneno ya kumkatisha tamaa kwa mtoto kwa kumwita majina kama vile "mbwa, mjinga" na mengineyo mabaya. Aweza kuyaamini haya na utakuwa umemwangamiza.

Watu wazima au watoto waweza kufanya vitendo vya kijinga, ila hii haimaanishi ni wajinga. Kama twaweza kuwaambia watu fulani maneno matamu, basi tujifunze hayo kwa wote, au tunyamaze kimya. Pia kusengenya watenda kazi wa Mungu mbele ya watoto, ni kujilaani. Japo watenda kazi hao ni watumishi waovu, hayo yazungumzwe na watu wazima tu! Kwa vile kwenye mawasiliano ni 7% tu hubebwa na maneno wakati ile asilimia 93 hubebwa na mkao wa sauti yetu na macho yetu. Tukumbuke mara zingine hatuna haja ya kusema ila tunavyomkodolea mtu macho, au mwonekano wetu tunakuwa tumempa mawasiliano mazito kuliko hata maneno yetu.
Dini iliyo safi, isiyo na taka ni kujilinda na dunia pasipo mawaa hasa ya mazungumzo ya ovyo. Wanyama na vitaambavyo kama simba, tembo na nyoka, vimeweza kufugika ila ulimi haufugiki, ni sumu kubwa. Tujiangalie tunayozungumza, tusiwe tuna maneno mabaya saa hii, na mazuri saa ile nyingine. Kinywa kimoja hakifai kutoa machungu na matamu. Ulimi waleta wivu na magomvi na machafuko, na Shetani apenda kukaa mahali hapo. Siku hizi kuna teknología na twaweza kuongezea tuwe waangalifu kwa yale tunayoandika kwenye kompyuta au simu kwa watu. Picha tunazoposti n.k.

Twaandika kwa hasira au bila kufikiri, hivyo ni vyema tungoje kwanza hasira ipoe, na kutuma barua hizi baada ya kuzicheua. Kwenye Waefeso 4:29 Paulo atukumbusha uchafu umo ndani ila tusiache utoke nje kupitia vinywa vyetu! Yaani tumwombe Mungu asafishe mawazo yetu, kisha hata maneno yatakuwa safi. Yakobo asema tusiwe watu wenye upendeleo; mtu akiingia kanisani ana pete ya dhahabu na mavazi mazuri na mwingine nguo mbovu; tunampatia yule mwenye uwezo, akae kiti cha mbele, na yule masikini akae chini. Hiyo ni hitilafu.

Mungu amechagua masikini wa dunia kuwa matajiri kwenye ufalme wa mbinguni. Kutimiza sheria ni kupenda watu, yaani majirani zetu. Tukitenda sheria yote, tukaacha moja ni sawa na kuwa tumekosa juu ya yote, maana Yeye aliyesema usiibe,

Ndiye aliyesema usiue pia. Imani iendane na matendo, maana mtu akimwona mtu asiye na nguo na chakula na kusema 'nenda kwa amani, ukaote moto na kushiba' atakuwa amemsaidiaje mtu huyo? Hata Ibrahimu alihesabiwa haki kwa imani, ila alionyesha aliamini yale Mungu anayomwambia akatii na kumtoa mwana wake Isaka.

Anazungumza vita na magomvi yatokana na tamaa, Mungu hatupi kwa vile hatumwombi, au tunamwomba vibaya. Tumpinge Shetani naye atatukimbia, tumkaribie Mungu, naye atatukaribia, tujinyenyekeze mbele za BWANA naye atatukuza. Yakobo anatukumbusha kwamba tukisema tuna imani, au twamini Mungu, ila matendo yetu ni maovu, kama ya watu wa dunia waovu, basi tu sawa na watu makafiri au mapagani wasioamini au pengine tu wabaya zaidi, kwa vile wao hawana nuru kama yetu. Basi dini ya kweli ni kusadia wajane, yatima, maskini, wageni na wale wenye mahitaji, na kujilinda na mawaa.

Yakobo anashauri kwamba tusipange ya kesho. Maisha yetu ni mvuke wa kitambo. Tusijisifu kesho nitafanya makuu, nitanunua nyumba ile, nitalima shamba hili, nitafaulu mtihani fulani. Tudumu kutenda wema, hasa kwa vile tumejua wema na ubaya maana yeye anayejua kutenda mema na asiyatende, akifikiri ndiyo imani, ametenda dhambi. Imani pasipo matendo imekufa. Anawapa Ole matajiri walie, na kupiga yowe maana mashaka na hofu zinawajia kwa kudhulumu watu wanaowafanyia kazi.

Waajiri wanaajiri watu na kuwalipa pesa ndogo, na wao wanajilimbikizia pesa nyingi. Kazi haziwi na marupurupu kama kutibiwa, pensheni au kusaidia watoto wao kwenda shule, hata kama hilo lina uwezekano. Matajiri hawa huchukua faida yote kwa matumizi yao wenyewe. Huwanyanyasa watenda kazi, wengine hata ni watoto wadogo, hawapewi elimu yoyote, japo watoto wao wanaenda shule za aghali sana. Mungu anasema dhahabu zao na fedha itaingia kutu, na hiyo kutu itakula miili yao kama moto kwani Mungu hataki dhuluma. Sisi sote ni watoto wa Mungu, hatuwezi kunyanyasa watu wanaotufanyia kazi, wawe mayaya, wakitufanyia kazi usiku mzima na kuamka asubuhi na kuendelea kufanya kazi, huku watoto na jamaa zetu wamestarehe, na wao wakiwatumikia wakiwa wenye huzuni kwa ajili ya suluba. Vilio vya watu hawa vimefika mbinguni. Ukweli wa dini ya mtu ni jinsi anavyowatendea watumishi wake na wanyama wake, iwe ni kupiga punda bila huruma, au kuwanyima watenda kazi wetu chakula cha kutosha nguvu za kufanya kazi nzito. Yakobo anamaliza akisema tusiwe na manung'uniko na kuishi maisha ya uovu, bali kama mtu amepatikana na baya aombe, ana moyo wa kuchangamka aimbe Zaburi. Na mtu anayeumwa aite wazee wa makanisa waombe na kumpaka mafuta maana kuomba kule kwa imani kutamwokoa yule mgonjwa, na BWANA atamwinua. Tukifanyiana baya tuombane misamaha.

Pengine siku moja mbinguni tutaona jinsi majaribu yetu yote yalivyounganishwa kwa ukaribu na wokovu wetu, na jinsi mateso haya mepesi yalivyotufanyia kazi. Mungu hutupatia hekima ya kutusaidia kustahimili majaribu kwa subira, akitupa fursa ya kuimarisha maeneo yetu yenye kasoro ya mazingira magumu, huku tukijifunza kuthamini utendaji unaofanana na kioo cha sheria ya uhuru, na hivyo

kutupa uwezo wa kuishi dini hiyo safi na isiyo na unajisi.

Maombi ya watu wanaompenda Mungu au watu wa haki yana nguvu nyingi, maana Eliya aliomba na mvua haikunyesha miaka mitatu na nusu, na akaomba na mvua ikaja tele. Mtu akiacha imani asimwamini Yesu tena, au asije kwenye ushirika tufanye bidii kumtembelea na kumtia moyo. Akirudi tena kwenye imani tutakuwa tumesaidia kuongoa roho. Ila tuwe na kukesha na kuomba, ili nasi tusianguke na kumfuata mtu huyo shimoni.

*Yesu Alikuwa na Mahali Mahususi pa Kuomba—Uwe na mahali pa sala ya siri. Yesu alikuwa na maeneo teule ya ushirika na MUNGU, na sisi pia tunapaswa kuwa napo/nayo. Tunahitaji mara kwa mara kujitenga hadi mahali fulani, hata kama ni panyenyekevu pa kiasi gani, mahali ambapo tunaweza kuwa peke yetu tu na MUNGU.

----------------------

Maswali: Kwa nini imani bila matendo imekufa? Ulimi una tatizo gani, usipotumiwa vizuri? Mtu akiumwa anashauriwa amwite nani? Matajiri wanaonyonya watu na kupunja watu mishahara wanapewa ole gani? Majaribu yana uzuri gani? Yakobo kama ndugu wa Yesu anaweza kujua mambo gani ambayo mitume wengine hawakujua? Ni watu gani walio na hekima wasiohitaji kuiomba kwa Mungu? Twawezaje kuwasiliana na mtu kwa kutumia macho, kubadilisha sauti au miili yetu? Twawezaje kuacha maneno maovu? Orodhesha maneno yanayoponya, na yale yayoua.

## SIKU YA 343.
## (Desemba 8)

**Waraka wa kwanza wa Petro**



Petro alikuwa mtume wa Yesu, na mmoja wa wale wanafunzi 12 wa Yesu. Alikuwa mmojawapo wa viongozi wa kwanza wa kanisa la Kikristo Yerusalemu. Aliwaandikia waumini hao akiwaambia wawe na furaha wanapoteswa kwa maana Kristo aliteswa kwa ajili yao, naye alipoteswa hakurudisha matukano. Yaonekana Petro alishuhudia hayo kwa macho yake. Alivutwa na upendo wa Yesu na akawa tayari kufanya lolote kwa ajili ya BWANA. Akakazia, ni bora kuteswa kwa kuwa umetenda mema, kuliko uteswe kwa sababu ya kuvunja sheria au kutenda uovu. Petro aliandika waraka huu akiwa Babeli na Yohana Marko akitukumbusha tumenunuliwa kwa damu ya thamani, na si kwa vitu viharibikavyo hivyo tuondoe hila na uovu wote. Anakazia tuwe makini mawazo yetu kuweka kwa vilivyo bora tu. Barua ya Petro ilikuwa kwa waumini wote kwa jumla, akiweka mkazo juu ya roho ya umoja na upendo, baada ya kuwa wametawanyika kutokana na mateso makali. Petro naye alijua mateso mengi, kwani alipigwa, alitishwa, na kupelekwa gerezani. Alichukulia haya bila kupata kinyongo wala kukata tamaa, bali aliendelea kumtii Mungu na kuishi maisha ya ushindi. Madhumuni yake ilikuwa kuwatia moyo wale wanaopata mateso kwa imani yao, na kuwataka waishi maisha ya utakatifu. Petro anasema kwamba utakatifu ni muhimu, hata wakati wa mateso na maumivu. Ni jambo la kawaida kwa waumini kuwekwa gerezani na hata kufa kwa imani yao. Petro anasema kila mtu awe tayari kushuhudia kwa mtu yoyote, lile tumaini lililo ndani ya moyo wake.

Hebu tuwe na kukesha maana mshitaki wetu Ibilisi ni kama simba angurumaye akimtafuta yoyote ammeze. Hivyo tuwe waangalifu na kukesha, tusimwachie mwanya na kujisahau tuko kwenye mapambano makuu. Petro anasema wakati wa mateso ni wakati wa kufurahi, maana tunashiriki mateso Naye. Mateso yaweza pia kuwa elimu na kutuonyesha dosari za kusahihisha kwenye tabia zetu. Uzima wa milele umeahidiwa kwa wale wote wampendao Mungu. Petro alifanya kazi na Wayahudi na hata watu wa mataifa akitembelea sehemu mbali mbali, hata alifika Rumi ile miaka ya 60BK kama vile Paulo alivyofika.

Zamani Petro alimkana Yesu bali alipata ujasiri na kuona ni bahati na heshima kuu kufa kwa ajili ya Kristo. Hata naye wanahistoria wasema aliuwawa na mfalme Nero kule Rumi kama Paulo. Japo barua hii ni fupi, ina mafundisho makuu ya imani. Anatusihi tunyenyekee daima chini ya mkono wa Mungu Naye atakukweza, tukimtwika Mungu fadhaa na matatizo yetu yote, maana Yeye hujishugulisha sana na mambo yetu. Tuishi maisha ya utakatifu maana imeandikwa "mtakuwa watakatifu kwa kuwa Mimi ni mtakatifu." Tumekombolewa na Yesu kwa damu Yake ya thamani, na si vitu viharibikavyo.

Basi yabidi tuweke uovu, hila, unafiki, husuda na masingizio yake yote mbali. Tukumbuke sisi ni wapitaji na wasafiri, hivyo tuepuke tamaa za mwili, yaani vitu tunavyoangalia na kutaka tuwe navyo, na mambo ambayo yanatufanya tuwe na kiburi na kujisikia sisi ni bora kuliko wenzetu, au kuliko Mungu Mwenyewe. Yesu ni Jiwe Hai, jiwe la pembeni, ambalo linahitajika kwenye kujenga nyumba iwe imara. Wote sisi ni wana wa mfalme, maana kwetu ni mbinguni, basi tuwe na mwenendo mzuri. Hebu watumishi watii mabwana zao, hata wale wakali, maana wakitenda mabaya wakapigwa makofi, ni haki yao, bali wakitenda mema, wakipigwa makofi au kupata adhabu; watakuwa wanateswa kwa ajili ya Kristo. Wanawake wawatii waume zao, maana ndiyo agizo la Mungu.

Petro anatoa mwongozo wa jinsi tunavyojipamba akisema, tusijiti nguvu sana kujipamba ili watu watuone, kwa kutumia mapambo ya nje tu, kama dhahabu, wigi, kusuka nywele au mavazi ghali ya kuvutia. Badala yake tujipambe kwa uzuri wa moyoni usioonekana ambao hauharibiki, yaani roho ya upole, utulivu, uvumilivu, na utii, hii ina thamani kuu mbele za Mungu. Hii haina maana tuvae nguo mbaya au chafu, la hasha. ila kamwe tusiwekee mkazo kujionyesha kwa watu, maana Mungu anajua yote yaliyo moyoni mwetu. Dhahabu, almasi na vito vingi ambavyo watu huvaa viliumbwa na Mungu na hata vitakuwapo mbinguni, ila shida ni vitu hivi vinapoonekana kuwa majaribu kwetu na kuvigeuza kuwa miungu. Sheria ya hili ni kutafuta kutumia pesa zetu, muda wetu na burudani zetu kwa utukufu wa Mungu.
Tukijipamba kwa kuweka heleni masikioni, au kwa kujionyesha inaharibu utu wa ndani, na hasa tunapogombana kuvilinda vitu hivi pale mtu anapojaribu kutusaidia, inaonyesha ni aina ya miungu fulani. Huu siyo wakati wa kuchukua pesa nyingi mno na kuweka kwenye mavazi, au kujipamba, hasa pale ambapo pana mahitaji ya kimwili, kihali na kiroho. Katika maisha yangu binafsi nimegundua mimi kama Mwafrika na mkristo daima ni fukara nisiye na pesa za kutosha hata kama ningekuwa bilionea. Nina ndugu wa kuwasaidia wengi. Kuna watu bilioni tatu ambao hawajapata injili kabisa katika dirisha la 10 kwa 40 lenye watu bilioni tatu

ambao hawajasikia habari za injili (1040window Joshuaproject.org).

Pia kila kukicha nakutana na watu wenye mahitaji mazito ya afya, mavazi, malazi au chakula. Wanapita mitaani wasio na viatu, nguo, wenye njaa. Siwezi nikachukua pesa na kuvaa suti, tai au vito vya dola 500 na nina ndugu wengi wanaangamia kiroho na kimwili. Huu ni ushuhuda wangu binafsi kwani nataka waishi milele, na si mimi nijitanue na kujiwekea kila kitu wakati ambapo kuna wengi hawajasikia kisa cha msalaba. Kuna watu watano waliojitoa mhanga kwa ajili yangu nilipokuwa gizani, ili nisikie habari hii njema ambayo karibuni inaenda kufungwa.
Huu ndiyo wakati wa kuwa kama mitume wa kuweka kila kitu kwenye madhabahu ili iwe sadaka ya kusaidia wengi wajitayarishe kwa ujio wa Yesu ambao upo mbioni. Hata hivyo kila kitu ni cha muda, labda miaka sabini au themanini ya binadamu, ila milele ni kuishi bila kikomo. Kadhalika wanaume waishi na wake zao kwa hekima, kwa kuwapa heshima kwamba japo ni wadhaifu kupita wao kimwili, ni warithi pamoja nao, wa neema ya uzima wa milele. Waume wanaonyanyasa wake zao, maombi yao yaweza yasijibiwe. Hili ni kwa wale wote walio chini yetu, tusipowajali, Mungu hatasikia dua zetu.

Watu wanaompenda Yesu ni lazima wapendane, wawe wanyenyekevu, na wasilipe ubaya kwa wema. Twapaswa kuwa watu tusiolaumu watu bali tuwe mbaraka. Kila mtu awe na juhudi katika wema. Si katika kupanga na kufanya uovu. Daima tuwe tayari kumjibu mtu ye yote atakayetuuliza imani yetu kwa upole na kwa unyenyekevu, si kwa kujisifu na mabishano ya dini. Hayo yatakimbiza watu. Waajiriwa wawaheshimu waliowaajiri, watoto wawaheshimu wazazi. Petro anamaliza kwa kuwasihi wazee wa makanisa wachunge kundi la Mungu. Walisimamie vyema, si kwa kulazimishwa au kwa sababu wanalipwa mshahara.

Wachungaji na viongozi wa kiroho, wasipende kupata fedha ya aibu. Tumeshuhudia watumishi wa Mungu wakiomba pesa kwa matumizi yao wenyewe. Wamewaambia watu watawaombea wakiwapa pesa kadhaa, au wakipokea rushwa kwa watu kwa kuuza 'maombi' wanayoombea watu. Wanauza vitambaa vya upako, mafuta ya upako n.k. Hili ni kosa. Washiriki na viongozi wao wajifunze kunyenyekeana na kuhudumiana. Mungu huwapinga wenye kiburi bali huwapa wanyenyekevu neema.

*Yesu Aliomba kwa Ajili Yetu—Mara nyingi Yesu alikuwa amechoka kutokana na taabu isiyokoma na kujikana nafsi (kujinyima), kujitoa mhanga, na kujinyima ili kubariki wanaoteseka na wahitaji. Alitumia usiku mzima katika maombi juu ya milima pweke, si kwa sababu ya udhaifu Wake na mahitaji Yake, bali kwa sababu Aliona, Alihisi, udhaifu wa asili zetu katika kupinga majaribu ya adui katika vipengele vile vile ambavyo vinatushinda sasa. Alijua kwamba tusingejali kuhusu hatari zenu na tusingehisi hitaji letu la maombi. Ilikuwa ni kwa ajili yetu ndiyo sababu Alimimina maombi Yake kwa Baba Yake kwa vilio vizito na machozi.
----------------------

Maswali: Petro aliandika waraka huu akiwa wapi? Kwa nini viongozi wa Kiroho wachunge vizuri kundi la Mungu? Kwa nini tunyenyekee kwa mkono hodari wa Mungu? Kwa nini wanaume waishi na wake zao kwa hekima?

**SIKU YA 343.**
**(Desemba 9)**

**Waraka wa Petro wa pili.**

Petro aliandika barua hii wakati anakaribia mwisho wa maisha yake, yaani kabla ya kuuwawa Rumi na Kaisari Nero. Petro aliona walimu wa uongo na manabii wafundishao mafundisho yasiyo na msingi wa Imani ya Kristo, wakiyaingiza mafundisho yao kanisani. Anawapa wosia Wakristo wakue kiimani na kuwa mashujaa ili waweze kutambua mafundisho ya uongo au uasi. Akasema walimu waongo wa dini hawa watajipatia faida kwa maneno yao yaliyotungwa.

Petro anatuambia hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, anapotujulisha kuhusu nguvu za BWANA Yesu Kristo, na kuja Kwake, bali ameuona ukuu wa Mungu kwa macho yake mwenyewe. Wakati Yesu alibadilishwa kwa ule mng'ao. Petro alikuwa karibu sana na Yesu akila Naye, akitembea Naye, na kwenda Naye pahali pote. Anasema alisikia yeye mwenyewe kutoka mbinguni ikisema "Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye."

Sauti hii waliisikia ikitoka mbinguni, akiwa pamoja na Yesu katika mlima ule mtakatifu, Yesu alipong'aa. Wote sisi Wakristo tumepewa Neno la unabii la Mungu lililo imara zaidi, yaani Maandiko. Maandiko taa ing'aayo mahali penye giza, tukiyaangalia, tunafanya vyema mpaka kutakapopambazuka na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwetu, Yesu atakapokuja. Petro anatuambia kuwa Maandiko hayakuja kama apendavyo mtu tu, bali watu walioandika waliongozwa na Roho Mtakatifu.

Petro anatukumbusha kwamba "ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika walioasi, na waovu, bali walitupwa, katika vifungo vya giza walindwe hata hukumu ije. Hata wakati wa Nuhu aliwaangamiza wote akamwacha Nuhu mjumbe wa haki na wengine saba, alipoleta gharika. Sodoma na Gomora nayo aliihukumu na kuifanya kuwa jivu kwa moto, akamwokoa Lutu yule mwenye haki aliyehuzunishwa na uovu wa miji hiyo. Basi Mungu atafanya hivyo hivyo siku za mwisho.
Atawaokoa watauwa na majaribu na kuweka wasio haki katika adhabu akiwamo na Baalamu yule mwana wa Beori aliyependa ujira wa udhalimu. Watu wadhalimu ni kama visima visivyo na maji, na mawingu yanayochukuliwa na tufani." Wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya uovu wa dunia, na wakanaswa tena na kushindwa; hali yao ya mwisho inakuwa mbaya kuliko mwanzo. Hawa ni kama mbwa aliyerudia matapishi yake au nguruwe aliyeogeshwa na akarudi kujigaragaza tena matopeni.
Petro ananukuu mara 35 Agano la Kale. Petro alisikia watu wakisema BWANA anakawia kurudi mara ya pili. Akawaambia waumini "BWANA hakawii kuitimiza ahadi Yake, kama wengine wanavyodhani kwamba anakawia bali huvumilia, maana Hapendi mtu yoyote apotee, bali wote tuifikie toba. Siku ya BWANA itakuja kama Mwizi ajavyo kwa wale wasiokesha na kujiweka tayari. Siku hiyo ya kuja Kwake kutakuwa na mshindo. Mbingu zitatoweka, na kazi za mikono ya binadamu

zitaunguzwa.
Basi imetupasa kuwa wenye mwenendo wa utauwa, tukiitazamia ile ahadi Yake ya mbingu mpya na nchi mpya. Basi Kwa vile tunatazamia kuja kwa BWANA tufanye bidii ili tuonekane katika amani, na kuwa bila mawaa wala aibu mbele zake. Tuendelee kukua katika Neema, na katika kumjua Yesu Mwokozi Yesu Kristo." Twapaswa tujifunze na kufanana Naye siku hadi siku. Mungu anataka tusonge mbele, na anatuwezesha kufanya hivyo. Tukiziamini ahadi za Mungu, atatusaidia zitimie katika maisha yetu. Hivyo kuja kwa Yesu kwetu hakutakuwa kama ujio wa mwivi. Je, uko tayari kumlaki Yesu mawinguni?

Je, umeshawahi kusikia ngazi ya Petro? Tukitaka kutumia ngazi tunaanzia chini kwenda juu. Ndivyo katika maisha yetu ya ukristo. "Kwa sababu hiyo, fanyeni bidii ya kuongeza fadhila katika imani yenu: ongezeni elimu katika fadhila yenu, kuwa na kiasi katika elimu yenu, uvumilivu katika kuwa na kiasi, uchaji wa Mungu katika uvumilivu wenu, udugu katika uchaji wenu, na upendano katika udugu wenu. Mkiwa na sifa hizo zote kwa wingi, zitawawezesheni kuwa watendaji na kupata faida katika kumjua Bwana wetu Yesu Kristo.

Hakuna njia ya kuthibitisha imani ya kweli bila majaribu, na imani ya kweli pekee ndiyo imani inayookoa. Je, uko kwenye majaribio ndani ya tanuru la moto sasa? Kumbuka Mungu wetu Ndiye Bwana Mwokaji Stadi: Atahakikisha umeokwa vizuri bila kuchomwa au kuunguzwa! Kuna tofauti kati ya yale ya muda na ya milele. Waumini walioandikiwa barua hii ni wageni, wakaaji wa muda na wahamiaji, huku wakingojea urithi wao wa milele. Majaribu wanayopitia ni ya muda tu, lakini kuna shangwe kuu mbele na baadhi ya hayo yanaweza kupatikana hata sasa, katikati ya majaribu. Kulikuwa na wale ambao hawakuwa wameelewa uhalisi wa kazi ya Mungu na upendo Wake, lakini sasa Yesu amefichuliwa kikamilifu. Maisha yetu ya kibinadamu ni dhaifu na yanapita, lakini maisha ambayo msingi wake ni Neno la Mungu yataendelea milele.
Lakini mtu asiye na sifa hizo ni kipofu, hawezi kuona na amesahau kwamba alikwisha takaswa dhambi zake za zamani. Kwa hiyo basi, ndugu zangu, fanyeni bidii zaidi kuufanya huo wito wenu mlioitiwa na Mungu uwe jambo la kudumu katika maisha yenu; kama mkiishi namna hiyo hamtaanguka kamwe. Kwa namna hiyo mtafaulu kupewa haki kamili ya kuingia katika Utawala wa milele wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo.

Kanisa linajaribiwa na mafundisho ya uongo hivi leo. Usalama wetu upo kweye Maandiko tu. Kila mtu yapaswa ajue kutambua mafundisho ya uongo na ya Kweli, ili aepuke shida. Ili kugundua noti bandia, hatujifunzi noti bandia, bali noti halali, kadhalika ili kugundua mafundisho ya uongo, tunasoma Biblia, ili yajapo mafundisho ya uongo, tuweze kutofautisha. Shetani, kupitia mawakala wake, manabii na walimu wa uongo, amekuwa akilishambulia kanisa la Kiristo kwa muda mrefu. Ameanzisha uzushi ambao wengi wameuingiza kanisani. Mojawapo ya hayo ni uibukaji uliofanywa na Mungu! (theistic evolution) ambayo yasema Mungu aliumba ulimwengu kupitia uibukaji, na mwingine ni kunyakuliwa, yaani watu watanyakuliwa kisiri kwenda mbinguni, Mafundisho haya ni mapya kabisa, na yameingia hivi karibuni tu. Wasomi wengi wa Biblia wanaamini haya na kisha

wanafundisha watu. Fundisho lingine hatari ambalo Wakristo wengi wamekubali ni fundisho kwamba roho huachana na mwili wakati wa kufa, na huenda kuzimu au mbinguni na kuwa hai huko, nje ya mwili (angalia Ezekieli 18: 4). Tena lingine ni kwamba siku ya kwanza ya juma, wala si siku ya saba, ndiyo siku ya kutakasa, Mungu alishuka binafsi katika mlima wa Sinai, na akasoma masikioni pa wanadamu, na baada ya hapo akaiandika kama moja ya Amri Zake Kumi, kwenye Mbao za mawe, kwamba siku ya saba ya juma, ndiyo siku ya kuitakasa (Angalia Kutoka 19, 20), na ambayo Yesu aliithibitisha kwa kuitakasa (Angalia Luka 4:16).

Katika siku hizi za mwisho, manabii wa uwongo wamekasirika zaidi. Watu wengi hata watoto wadogo wanasema wao ni manabii au ni mitume, na wanawaambia watu walete pesa. Mambo haya yalikuwa hayapo mengi ila siku hizi yamejaa kila mahali. Watu wameona huo ndiyo mradi wa kujishibisha matumbo yao. Bwana wetu Yesu ametuonya akisema, "Kwa maana watatokea Wakristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule." Mathayo 24:24. Shetani anadanganya ili kuharibu. Ni kupitia tu uhusiano wa kibinafsi na Yesu, na ujuzi wa Neno lililoandikwa ndipo tunaweza kuepuka kudanganywa. Kwa hali hii, acha Roho Mtakatifu awe Mwalimu wetu tunapojifunza Biblia.

*Wanafunzi wa Kristo walivutiwa sana na maombi Yake na tabia Yake ya ushirika na MUNGU. Siku moja baada ya kutokuwepo kwa Mola wao kwa muda mfupi, walimkuta amezama katika maombi. Akionekana kutojua uwepo wao, Aliendelea kuomba kwa sauti. Mioyo ya wanafunzi iliguswa sana. Alipomaliza kuomba, wakasema, "Bwana, tufundishe kuomba."
------------------------

Maswali: Mtu gani anafananishwa na nguruwe aliyerudi kujigaragaza topeni? Ni nini usalama wetu kuepuka mafundisho ya uongo? Sema visa vitatu vya Agano la Kale ambavyo Petro amenukuu? Maandiko yalikujaje kwetu?

**SIKU YA 344.**
**(Desemba 9)**

**Waraka wa Yohana wa kwanza.**

# Tazameni pendo la ajabu! Mungu ni Upendo.



Yohana alikuwa 'mtume mpendwa' na mdogo kwa umri kwa wote. Aliona kubadilishwa kwa Yesu kwa mng'ao, na akashuhudia Eliya na Musa walipokuja kumfariji Yesu. Huyu ni shahidi aliyeona mambo kwa macho yake mwenyewe. Yawezekana alikuwa na ujamaa wa karibu na Yesu, hasa upande wa mama yake, kutokana na Marko 15:40, Mathayo 27:56 na Yohana 19:25-27. Mama yake Salome, alikuwa na undugu na mama ya Yesu.

Yesu alimkabidhi mamaye kwa mtume huyu na si kwa ndugu zake wa tumbo moja. Yohana alikuwa katika bustani ya Gethsemane na kushuhudia jasho na damu zikimtiririka Yesu. Yohana aliandika kitabu cha injili, yaani maisha ya Yesu na kitabu cha Ufunuo, ambacho kilikuwa ni maono katika kisiwa cha Patmo. Yohana alikuwa mtu mzima sasa akasema na washiriki wapenzi watoto wadogo. Yohana katika barua zake anatukumbusha upendo wa Mungu mkuu na kwamba sisi ni watoto Wake.
Mtoto yeyote anapouelewa upendo wa Mungu, atakuwa na furaha, shukurani na kumpenda Mungu na watu. Mungu anatujali sana na ndiyo maana anatutunza. Yohana anataka tukae karibu na Mungu. Hii itatusaidia kumtumaini zaidi. Alipofikia uzeeni Yohana aliishi Efeso. Pengine barua yake yahusu kanisa hilo. Kanisa liligawanyika, Yohana anaandika kusaidia kanisa ili kutofautisha mafundisho makuu ya imani ya uongo na yale ya kweli. Wengine hawakuamini kwamba Yesu ni Masihi, na kwamba hakuja katika mwili.

Wengine walisema hawamhitaji Yesu kama Mkombozi wao na mtetezi. Wakadai wana uwezo wa kuwa na uhusiano na Mungu moja kwa moja. Kitabu hiki ni muhtasari wa kitabu cha injili cha Yohana kwa namna fulani. Mzee wa Imani Yohana alitaka watu washikilie imani, maana kutoka katika imani ni giza kuu. Mungu ni Mwanga, wala giza lolote halimo ndani yake. Leo kuna mafundisho ya giza ya imani, kushinda siku za Paulo. Mafundisho ya miungu ya uongo. Tukumbuke Mungu ni mwanga ndani Yake hamna giza kabisa.
Tukisema kwamba tunashirikiana Naye, ila tunaenda gizani tunajidanganya, wala Kweli haimo ndani yetu, kwani tu waongo tu. BWANA anatuambia hata kama tumetoka kwenye mstari "tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata, atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote. Ila tukisema

hatukutenda dhambi twamfanya Yeye kuwa mwongo wala Neno Lake halimo ndani yetu.

Yohana anawaambia watoto wadogo, nasi wote tulio watoto wa Mungu, tusitende dhambi, bali tukitenda dhambi tuna mwombezi kwa Baba. Anayetuombea na makosa yetu yanafutwa. Kumjua Mungu ni kuenenda katika njia yake, tukishika Maagizo Yake, yaani Maandiko Yake. Hatuwezi kusema tunamjua na kumpenda Mungu na kujifanyia tunavyotaka. Hata watu wanaotuona watasema "Watu hawa wana porojo, na wanaishi maisha ya unafiki."
Yohana anasema hatuandiki amri mpya bali ile ile ya Upendo. Tusichukie watu, maana yeye amchukiaye ndugu yake yumo gizani na wala hana nuru. Yohana anaandikia barua watoto wadogo, kwa sababu dhambi zao zimesamehewa, kwa Jina la Yesu na sasa wanamjua Baba. Kisha anawaandikia wakina baba kwa kuwa wamemjua Mungu toka mwanzo. Mwisho anawandikia vijana kwa vile wana nguvu na wamemshinda yule mwovu, na Neno la Mungu linakaa ndani yao. Habari hizi zinatia moyo.

Yohana alitaka kuwaonyesha waumini wawe na uhakika wa asilimia 100 kwamba imani yao na matumaini kwa Yesu yatawafanya wakae Naye milele zote. Anatuonya tusipende dunia na mambo yake. Tamaa ya vitu vya dunia haitokani na Mungu. Dunia inapita pamoja na tamaa zake zote, bali yeye afanyaje mapenzi ya Mungu adumu milele. Mpinga Kristo anakuja wakati wa mwisho; ila wakati wowote duniani kuna wapinga Kristo. Kila amkanaye Yesu Kristo na kumkana Baba ni mpinga Kristo. Au yoyote ajionaye ni bora kuliko Mungu, basi ni mpinga Kristo, tunawezaje kujua kama tunajiona kwamba sisi ni bora kuliko Mungu basi? Tunamwomba Roho Mtakatifu atufunulie, maana hiyo ndiyo ilikuwa shida ya Hawa, aliona kwamba ni bora kuliko Mungu, na hivyo hakufuata maagizo aliyopewa.

Tusipoenda kutokana na maagizo ya Mungu, bali tunasema tunamwamini Mungu, tumekuwa wapinga Kristo. Kristo hakuwa mvunja sheria. Tuangalie watu wasitupoteze na mafundisho ya uongo yasiyo kwenye Neno la Mungu. Yohana anasema ni muhimu tujue kwamba Yesu si mtu mzuri tu! Bali ni Mwana wa Mungu. Yesu ni Mwanadamu na pia ni Mungu. Yohana aliandika kuhusu upendo wa Mungu tena na tena, na akatuagiza tupendane. Dini ya Kikristo bila Kristo kuwa Mungu inakoma kuwepo. Barua ya Yohana inatoa mwaliko kwetu sote kufurahia "ushirika" pamoja na Baba na Mwanawe, Yesu Kristo. Neno ushirika linazungumza juu ya ubia. Linarejelea watu wanaofanana kwa kitu fulani. Mwenyezi Mungu, kiongozi wa mbingu na nchi, anatualika tuingie katika ushirika pamoja Naye!

Ili nuru yetu iangaze, tunapaswa kuungama dhambi zetu kwa dhati, na kumwomba Mungu atutakase kutoka kwazo. Tukiangalia vizuri, tutaona kwamba tuna dhambi za kuungama na kusafishwa nazo. Inaweza kuwa dhambi ya kukosa subira, dhambi ya kutilia shaka ahadi za Mungu, ubinafsi au kiburi. Kwa ufupi, kwa kuwa hatufanani kabisa na Yesu katika tabia, tuna dhambi za kuungama, na kusafishwa kwazo. Tuombe Mungu atupe dawa ya macho tunayoihitaji ili tujione jinsi anavyotuona.
Yeye alipoanza kuwa na Yesu alikuwa na hasira, akitaka awe mashuhuri na kuheshimiwa, akipenda kulipiza visasi, ila alibadilishwa na upendo wa Yesu.

Alimpenda Yesu ila alikuwa na mikwaruzo, naye alikuwa tayari kubadilishwa. Je, Wewe u tayari kubadilishwa leo ufanane na Yesu? Yesu anatuonya kwa sauti ya Roho Wake Mtakatifu kama vile alivyokuwa anamwonya Yohana. Yohana Anakazia tusipende kwa maneno tu, bali kwa matendo. Anasema "tazameni ni pendo la namna gani alilotupa Baba kwamba tuitwe wana wa Mungu, na kuwa wana wa Mungu ni kuwa na tabia ya Mungu na atakapodhihirishwa kwetu tutafanana Naye." Mtu anayekaa katika Yeye hatendi dhambi, na akitenda huungama na kujutia na kutafua njia Yake. Tusistaajabu ulimwengu ukituchukia. Mungu alitupenda sisi kwanza, na si sisi tuliompenda kwanza.

Hatuwezi kumpenda Mungu tusiyemwona, na tukamchukia binadamu tunayemwona, hivyo anatuhimiza tupendane sisi kwa sisi kwanza. Mungu anatupenda sote ndiyo maana alimtoa Mwanawe wa pekee afe kwa ajili yetu. Yohana ameandika Maneno ambayo mara nyingi tumesoma "MUNGU NI PENDO!" Neno hili upendo, tunalolitumia kuelezea vile Mungu anavyotujali ni jitihada hafifu za kibinadamu kuelezea ukweli juu ya Mungu anavyotujali.

Wataalamu wa lugha na Biblia wanasema neno upendo, linasimamia zaidi ya sifa au tabia 23. Zikiwemo rehema, neema, haki, uvumilivu, fadhili, wema, faraja, tumaini, amani na kadhalika. Tuziepuke roho za uongo, maana zimeshakuja tayari, na zitaendelea kuja kupitia kwa manabii wa uongo. Tuzipime roho hizo kama zinamkiri Yesu ni Mwana wa Mungu, la sivyo roho hizo ni za mpinga Kristo. Watoto wadogo anasema Yohana "tukiomba sawa sawa na mapenzi yake, Mungu atusikia, basi tuombe kwa ujasiri.

*Yesu Alipiga Magoti Alipoomba—Katika ibada ya hadhara na faraghani, ni fursa yetu kupiga magoti mbele ya Bwana tunapotoa maombi yetu Kwake. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Juu ya wanafunzi Wake imerekodiwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akaomba, akashukuru mbele za MUNGU wake."
-----------------------------

Maswali: Kwa nini Yohana aliandika barua? Kwa nini tusipendane kwa maneno bali kwa matendo? Kuwa wana wa Mungu ina maana gani? Amchukiaye ndugu yake yupo wapi? Kwa nini ni muhimu kupenda watu hata kabla ya kumpenda Mungu? Mungu ni upendo ina maana gani? Je, ni nini kilisaidia kutoa radi au hasira za Yohana "mwana wa Ngurumo"?

## SIKU YA 345.
## (Desemba 10)

**Waraka wa Yohana wa Pili**

Yohana anatuma barua kwa Mama mteule, ujumbe mkubwa ukiwa "tupendane." Ujumbe wake wa dharura ni kuhusu waumini wenye mafundisho ya uongo. Si watu wa dunia, wenye mafundisho ya ulaghai, bali waumini. Mafundisho ya watu wa dunia utayagundua mapema na kuyaepuka, ila ya waumini, yahitaji hekima kuyapembua maana yana ukweli mwingi, na uongo mchache. Wadanganyifu wengi wametokea duniani wasiokiri ya kuwa Yesu Yuaja katika mwili. Yesu ameshautwaa ubinadamu milele! Anasema udanganyifu huu ni wa Mpinga Kristo.

Mara nyingi udanganyifu huu unaharibu kanisa kwa kiasi kikubwa kwa vile unatoka kwa viongozi wa kanisa. Viongozi wanaangusha wengi kwa chachu yao na kwenda nao nje ya mstari wa Mungu. Mafundisho ya uongo, au elimu ya uongo mara nyingine inatoka kwa watu wa karibu toka kwetu. Kwa maisha yao au kwa kufanya vitu, wanatuashiria kwamba kumcha Mungu si kitu cha kukitafuta kwanza, nasi tunaamini yale. Mara zingine watu hawa humsikia Roho wa Mungu na kujirudi na hatimaye kupona, na kukaa katika imani tena. Ila wale wanaowaongoza wanakuwa wameenda mbali na wanashindwa kurudi nyuma.

Mama mmoja aliyeolewa alisema kwamba yeye hawezi kufanya Mwenyezi Mungu anavyotaka, kwa maana mume wake aliingia mafundisho ya uongo. Akaacha kuja ibadani na kusema wakae nyumbani na kufanya matengenezo, maana kushirikiana na waumini wengine si muhimu maana hao waumini wengine ni Babeli au machafuko. Walipokaa nyumbani walichoka, wakaacha ibada waliyokuwa wanafanya nyumbani, na siku ya BWANA ya kuabudu ikawa ya kawaida tu bila ibada yoyote. Walianza kugombana wao kwa wao, na hata watoto wao waliacha imani.

Mwishowe yule mke alifariki, na inavyojulikana alipotea kwani hakuna aliyeshuhudia mabadiliko yake ya kuungama au akijirudi mwenendo wa zamani, japo ni Mungu Ndiye anajua mwisho wake. Mume wake baada ya miaka mitano aliamua kurudia imani, na kurudi kumpenda Mungu kwa upendo wake ule wa kwanza. Wengi walijiuliza, itakuwaje siku ya hukumu, maana alikuwa na msimamo mzuri walipofunga ndoa ila mume akampoteza. Na Sasa mume alirudi na yule mama hakupata nafasi. Kweli bahati ya mwenzako usilalie mlango wazi. Jambo hili lilitokea kwa mfalme Manase. Alipotosha Maelfu kwa ibada za uongo, ila mwisho alipata nafasi ya kutubu baada ya kuchukuliwa mateka. Alimrudia Mungu japo alipotosha wengi.

Mafundisho ya uongo ni pamoja na kutia chumvi kwa mambo, au kusema mambo ambayo tunajua si ya kweli yote. Mara zingine kwenye mazishi ya mtu, watu wamesema vitu kama "ndugu yao ataenda mbinguni" wakati walijua kwamba alikuwa akitendea watu mengi maovu. Hakuna anayesema mabaya kuhusu mtu

aliyekufa, na hili ni sawa, ila kama mtu aliyekuwa na matendo maovu ya wazi ni bora kunyamaza kuliko kumsifu kupingukia na kusema kwamba ataenda mbinguni na maisha aliyoishi yalikuwa kinyume cha imani. Basi marafiki zetu wakiwa wana pumzi bado, tuna nafasi ya kuwaambia waishi iwapasavyo, iil mtu anayempenda Yesu asije kusema uongo kwenye mazishi yake ili kuvutia mazungumzo, huku tukijua fika ameishi maisha ya kumtukuza Shetani.

Mafumbo matatu yatatupa mshangao kule mbinguni, moja-Nimefikaje hapa mbinguni jamani, ni maajabu maana mara nyingi nilianguka dhambini. Mbili-wale niliowategemea kuwepo mbinguni, mbona siwaoni hapa? Tatu- Wale ambao nilifikiria wataenda motoni, mbona nawaona hapa mbinguni!

Yohana anasema mtu akija kwetu naye haleti mafundisho ya Kweli bali analaghai watu, basi huyo "msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu." Maana ukimpa salamu mnashiriki kazi zake mbovu. Maneno haya ni mazito, mara nyingi sisi huwa tunakenua meno na watu hawa na kuendelea kusikia ulaghai wao, tukipoteza muda wetu. Runinga, Kompyuta na vifaa vingine vya teknolojia ya habari vina maarifa, na elimu nyingi za uongo, hivyo panahitajika kuchuja mno yaliyomo humo, hasa kwa watoto. Mtu anayempenda na kumtafuta Mungu aepukane na mambo ya kupoteza muda. Kupoteza muda kwa njia ya shughuli nyingi ni moja ya malengo ya Shetani ya kututoa kwenye mstari wa mafanikio kiroho na kimwili. Hasa kwa vyombo vya kisasa kama video, simu, kompyuta na vingine vya umeme!

Miaka ile pia yaliyotokea mafundisho ya uongo yaitwayo Gnostic. Watu waliamini wokovu watokana na elimu au maarifa. Waliamini kwamba roho ni takatifu na njema wakati wote, ila mwili ni mwovu. Ubinadamu wa Yesu ulikataliwa, kwani waliamini mwili ni mwovu. Walisema mwili utendewe kwa ukatili. Watu hawa waliamini kwamba mwili na roho ni vitu viwili tofauti, roho ina nafasi ya kuishi tena kuliko mwili, hivyo unaweza hata kuutesa mwili, maana hauna thamani kubwa, hiyo ilikuwa imani yao potofu. Yohana anaitwa mtume wa upendo. Anasisitiza tupendane, kwa sababu Mungu ni upendo. Naye apendaye ni mwana wa Mungu, na anamjua Mungu.
Haiwezekani kuwa na upendo usio na ubinafsi ambao Biblia inatuagiza kuwa nao bila Roho Mtakatifu. Uthibitisho kwamba mtu amejazwa na Roho Mtakatifu ni uwezo wake wa kupenda (Angalia 1 Yohana 4 : 12, 13), kwa maana upendo ni tunda la Roho Mtakatifu (Angalia Gal. 5 : 22, 23). Ni kwa tunda hili ndiyo tunawajua watoto wa Kweli wa Mungu.

Shetani atajaribu kuwadanganya, ikiwezekana, hata wale wateule (Mt. 24:24). Udanganyifu katika siku hizi za mwisho unahitaji neema ya Mungu, na ujuzi mzuri wa ile Kweli ili kuuepuka. Je, unaweza kuamini kwamba katika saa hii ya mwisho ya historia ya dunia, Wakristo fulani hawaamini tena Utatu? Baadhi ya Wakristo wazuri wa zamani sasa wanaamini kwamba Mungu alichukua mamilioni ya miaka kuumba ulimwengu wetu kupitia uibukaji. Mwanaume wa Scotland Yard aliulizwa jinsi walivyoweza kugundua sarafu bandia, akifikiri kwamba walichunguza sarafu nyingi za bandia. Lakini mwanamume huyo wa Scotland Yard alijibu kwamba, badala yake, walitumia muda wao wote kusoma fedha halisi vizuri sana hivi kwamba wakati wowote sarafu ya bandia ilipowekwa kando yake, tofauti ikawa wazi. Hivyo

ni lazima tujue ukweli uliomo katika Biblia, ili wakati wowote mafundisho yenye makosa yanapowekwa kando yake, tofauti itakuwa wazi. Hilo linahitaji kujifunza Biblia kwa bidii, dhati na maombi mengi.
Tusipopenda au kuwa na upendo basi hatumjui Mungu. Yohana ana mambo mengi ya kutuambia, ila anaishia hapo kwa hii barua fupi.


*Maombi ya faragha, maombi ya Familia, maombi katika mikusanyiko ya hadhara kwa ajili ya kumuabudu MUNGU, yote ni ya muhimu. Na tunapaswa kuyaishi maombi yetu. Tunapaswa kushirikiana na Kristo katika kazi Yake.
-------------------------

Maswali: Yohana anatuma barua kwa nani? Kusudi kubwa la Yohana kwenye barua hii ni nini? Je, katika shule au nyumba yako kuna mafundisho gani ya uongo yasiyoendana na Neno la Mungu? Je, twawezaje kuwa na upendo wa Mungu bila kuchuja mafundisho makuu ya imani? Je, twawezaje kuepuka upendo wa maneno matupu? Je, twaweza kumpenda Mungu bila kuzitii sheria Zake?

**SIKU YA 346.**
**(Desemba 11)**

**Waraka wa Yohana wa tatu.**

# Naomba ufanikiwe katika mambo yote.



Yohana anaandika barua hii, kumtia moyo mtenda kazi mwenzake Gayo katika huduma anayofanya. Asema "Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo." Kuwa na afya ya mwili kunatusaidia kuwa na afya ya kiroho. Neno 'Desozo' la Kiyunani linasimamia afya na wokovu pia. Tukiwa na afya na kuishi miaka 70, ni jambo dogo kulinganisha na wokovu, maana ni kuishi milele. Kupitia ubongo wetu ndivyo tunavyopata kumjua au kumwelewa Mungu. Hatujui mengi kuhusu Gayo, ila tunajua kwamba Yohana alimpenda sana! Gayo anasifiwa pia kwa karama ya kukaribisha wageni na ukarimu.

Mfano endapo tunavuta sigara, na kunywa pombe au kufikiri mawazo machafu, haya yanaharibu bongo zetu na kufanya tusielewe Neno la Mungu au mpango wa Mungu kwetu. Ubongo ndiyo yapo mapambano kati ya malaika wa Mungu na Shetani, maana kupigana kwetu si kwa nyama na damu. Wanasema kwa wastani watu wanaanza kuvuta sigara au kileo huanza wakiwa wadogo au pungufu ya miaka 15. Tukiwa wagonjwa ni vigumu kusaidia wenye shida, maana sisi wenyewe ni wahitaji, na mara nyingi tunakata tamaa, na kuchoka-choka tukiwaganda watu watusaidie.

Hata hivyo hatuwapi watu wasiomjua Mungu picha nzuri kama tunafanya vitu vibaya vya kuumiza afya yetu, maana tuliambiwa tusiue, hii ni pamoja na kuepuka kuutendea mwili vibaya. Kila kifaa kinapotoka kiwandani huja na kanuni ya kukitumia. Hata miili yetu Mungu ametoa kanuni za kufuata, na kanuni hizo zipo kwenye Biblia. Huwezi kuweka chumvi kwenye tanki la Petroli bila kutegemea kuharibu gari. Vivyo hivyo nasi tusiingize kila kitu tu mdomoni. Vyakula vinavyoitwa makapi ambavyo si salama kwa afya yako usile. Hivi ni vile vyenye sukari nyingi, mafuta mengi au vilivyokobolewa. Pia ni vyema kula mara mbili kwa siku chakula bora, cha nafuu na unacholima, chenye ladha nzuri, na kinachopatikana kirahisi. Kama unafanya kazi za mazoezi makali kama kulima waweza kula mara tatu, ila

watu wachache sana hufanya kazi nzito. Mtu anayekuja kama saa nne na saa kumi hivi, ana ratiba nzuri.

Sukari imekobolewa yaani maji ya miwa yamepunguzwa lishe au thamani yake. Mafuta nayo yamekobolewa. Epuka kula vyakula vya kuigiza vinavyooneshwa kwenye runinga, bali kula vile Mungu alivyoviumba yaani vyakula vya asili. Inachukua mahindi 14 yaliyo kwenye magunzi kupata mafuta kijiko kimoja kikubwa. Ilikuwa mpango wa Mungu ule mahindi 5 ushibe, ila ukila chips sahani moja unakuwa umekula mahindi 28 hivi. Vyakula vilivyokobolewa ni vina thamani ndogo na havishibishi ila vinawakilisha chakula kingi.

Mfano mwingine ni jibini. Kipande kidogo kama kiganja cha mkono, chapatikana kutokana na maziwa lita 20 hivi, hii ni kupoteza chakula, na kula vyakula vya kunenepesha. Kamwe usikoboe mahindi. Tumia ngano na ule mchele wa kahawia. Jifunze tiba rahisi utumie wakati wote. Jifunze kutofautisha pa kutumia tiba rasmi ambayo ni ya muhimu maana ina vipimo vinavyotusaidia mno, na mara nyingi ni msaada mkubwa kwenye dharura. Tiba rasmi na tiba mbadala zote zimetajwa kwenye Maandiko Matakatifu.

Biblia ina matabibu rasmi na mbadala. Hawa wote wapaswa kufanya kazi pamoja bila uchu wa pesa, bali kwa kusaidia na kuhudumia watu wa Mungu. Watu wanaompenda Mungu, wakiwa kwenye tiba rasmi au mbadala, watajitahidi kutafuta namna ya kupunguza gharama za matibabu, kuboresha afya na kupata riziki pia. Tutazungumzia mambo kumi hapa ya afya ambayo ni muhimu "kufanikiwa kimwili na hata kiroho." Mambo haya yaitwa 'Matabibu kumi'.
Haya ni mambo rahisi ambayo Muumba alitupa ili tuweze kuyafanya wenyewe, kila siku ikiwa kama kinga ili tupunguze magonjwa. Wazungu Hutumia maneno
NEW START --yaani
Nutrition (lishe),
Exercise (Mazoezi),
Water (Maji),
SUN (jua),
Temperance (Kiasi),
Air (Hewa bora),
Rest (Mapumziko),
Trust in Divine Power (kumtegemea Mungu),
Mengine ni
Moyo wa kusifu na shukrani, kutolalamika, Usafi, Kazi, Mtazamo, Kuhudumia, ujasiliamali na Kilimo.
Katika Kiswahili tutayaweka kwa mpango usio na maana ila itatufanya tukumbuke, waweza kuyapanga unavyoweza kuyakumbuka.

**MAKUNDI 10 MUHIMU KWA AFYA YAKO**

1. Maji: Ni muhimu kunywa maji glasi 4 kwa mtoto, na glasi 8-12 kwa mtu mzima kwa siku. Maji yanasafisha mwili ndani, na nje kwa kuoga na ndani kwa kukanda mwili na kunywa. Usinywe maji na chakula, acha saa moja mpaka mawili. Jitahidi kupata maji bora, yachemshe na kuyachuja. (Soma zaidi jinsi

ya kutumia maji moto, vuguvugu au barafu kwa kukanda).

2. Jua: Twapasa kupata jua angalau saa moja kwa siku. Jua linasaidia vitamini D, Kupunguza kansa, na kuongeza kinga ya mwili.
3. Kumtegemea Mungu: Kumtegemea Mungu kunapunguza hofu, hasira, wasiwasi na kukata tamaa nayo inaongeza afya, kwani moyo uliochangamka ni zaidi ya dawa. Mungu Ndiye mponya, tukimwamini na Neno Lake, ni uponyaji tosha. Tutakuwa na dhamiri safi, zisizotushitaki, na kujua Mungu ametusamehe. Tutasamehe watu na kuomba msamaha tuliowakosea kwani kutosamehe ni kama kula sumu, tukitegemea mwingine atakufa. Tunapofanya baya inatubidi tujisamehe pia. Jua Mungu ana nia nzuri nawe. Epuka uovu wa uibukaji au ukafiri wa kusema sisi wanadamu 'tumetokana na nyani.' Wazo hilo halina msaada wa kiafya.
4. Lishe: Asilimia 80% ya matatizo ya afya yanatoka na lishe. Watu wengi wanaoenda kumwona tabibu, shida walizonazo zinahusiana na lishe. Vyakula vya muhimu vya kula ni vitano tu, navyo ni matunda angalau matano kwa siku, mboga mboga, nafaka zisizokobolewa, jamii ya maharage au dengu dengu, jamii ya karanga kama nazi, korosho, ufuta, au alizeti. Hivi vyapaswa kuliwa kila siku. Badilisha rangi tu! Mfano ugali wa ulezi, ugali wa mtama, maharage, njegere, kunde, kweme, choroko, nazi, karanga, korosho, nanasi, chungwa n.k. Kuwa na bustani ni muhimu kwa kila binadamu ili ale vyakula bora na pia ni mpango wa Mungu mtu asiwe masikini hata kukosa chakula hivyo kila mtu kwenye Maandiko aligawiwa kipande cha ardhi! Milo miwili kwa siku ndiyo bora, na inatakiwa ipishane angalau kwa masaa 5 hadi 6 ndiyo ule mlo mwingine. Katikati ya masaa hayo, usile kitu chochote hata punje ya karanga. Jaribu kula kwa kiasi. Uzito wako usiwe mkubwa. Siku hizi hata watoto wadogo hupata ugojwa wa moyo utokanao na unene. Bustani ya Edeni ilipotea kutokana na chakula, ukiweza kutawala nafsi yako kwa ulafi itasaidia kukuza mionjo ya kiroho. Funga mara moja kwa siku kama huna shida ya afya. Hata mambo ya kiroho kama kushinda majaribu itakuwa rahisi. Kumbukumbu la Torati 18 yasema mtoto mlafi alipigwa mawe akafa. Jaribu kula chakula chako angalau nusu kibichi, yaani matunda na mboga mboga kama kabeji, matango, nyanya, karoti, chakula kilichokufa (kilichopikwa) ni hafifu kushinda magonjwa; hata hivyo bustani ya Edeni haikuwa na masufuria.
5. Mazoezi: Angalau nusu saa mpaka saa moja kwa siku. Mazoezi bora ni kutembea, ila mengine ni sawa pia. Fanya mazoezi yenye faida kama kulima au kazi zingine badala ya kujikimbiza kimbiza bila faida, ila ukiwa mjini basi huna jinsi basi kimbia au nenda gym.
6. Hewa safi: Ni muhimu kuvuta pumzi vizuri kwa ndani, mara nne au tano kwa siku. Jaribu kukaa nje siyo ndani saa zote. Fungua madirisha ya nyumba, na usiwe na miozo ya vyakula, au pipa karibu na nyumba yako.
7. Kiasi: Kiasi ni kutotumia kamwe vitu vibaya kama sigara, pombe, kahawa au vile vingine; na kutumia kwa kiasi vitu vizuri, kama mboga au matunda. Tusiwe na ulafi wa chakula, kuvaa mno, kukarangiza sana, kutumia muda kwa kujiburudisha mno n.k
8. Mapumziko: Twapasa kulala angalau masaa 10 kwa watoto wa shule, nane kwa watu wazima, watoto wachanga mpaka 20 hivi. Twapasa kufanya kazi siku sita na moja kupumzika kama maagizo ya Biblia yasemavyo, ili kufanya

mwili usichakae, na kuwa na mawazo bora. Kuabudu hufanya mahusiano na muumba wetu yawe bora.

9. Huduma ya jamii: Kuhudumia watu na kuwajali inatusaidia mioyo yetu kuburudika, na kutoangalia mashida yetu kila mara, au kukata tamaa. Ni heri kutoa kuliko kupokea. Tumia muda wako kusaidia kazi nyumbani na kusaidia wenye mahitaji. Utakuwa na afya na maisha marefu.
10. Moyo ulio na shukurani: Watu ambao wana shukurani kwa Muumba na wamsifu wameonekana kuishi maisha marefu yenye afya kuliko wale walio na manunguniko na ulalamishi. Mtu akikutendea mema awe mzazi au mwalimu, kumbuka kushukuru, si haki yako. Mwandikie hata barua ukisema umetumiaje kile umezawadiwa. Utatia watu moyo, na wewe mwenyewe utapata kuvamiwa na tabasamu na furaha mara zote. Daima uwe na maneno yale matamu tunayojifunza tukiwa wadogo au chekechea. Maneno hayo ni ahsante, pole, samahani, tafadhali na naomba.

Kuna sehemu ya tiba rasmi na sehemu mitindo ya maisha yetu. Ila Kweli yote katika tiba ni kuponywa na afya zetu za kiroho. Hii inarejesha mahusiano yetu binadamu na BABA yetu wa mbinguni.

Yohana anamtahadharisha Mzee Gayo na tabia mbaya ya Diotrefe, aliyependa kuwa wa kwanza, na dikteta aliyechukua makanisa ya Asia. Huyu alikuwa na tabia za ovyo, ikiwemo na kusema maneno maovu na matendo ya upuuzi. Alikuwa hana ukarimu, kwani Hakukaribisha ndugu katika Kristo na wale wanaotaka kukaribisha wenye mahitaji aliwazuia. Yohana amwambia Gayo ambaye alikuwa mlei mwenye uwezo wa mali na mcha Mungu anayeishi mji wa Efeso asiuige huu ubaya bali auige wema, kwa kuonyesha wema kwa wote wanaofanya kazi ya injili. Atendaye mema ni wa Mungu, na atoa mfano mzuri wa Demetrio, ambaye anatenda mema, na hivyo amemwona Mungu. Anamaliza kwa kusema anatarajia kuwaona awasalimu, na kumtaka Gayo awasalimu wote kwa majina yao.

*Wote tunahitaji Kukesha na Kuomba Daima—Mwanzo kabisa wa uovu ulikuwa ni kupuuza kukesha na maombi ya siri, kisha kukaja. kupuuza majukumu mengine ya kiroho, na hivyo njia ilifunguliwa kwa dhambi zote zilizofuata. Kila Mkristo ataweza kushambuliwa na vivutio vya ulimwengu, usumbufu wa asili ya tamaa za kimwili, na majaribu ya moja kwa moja ya Shetani. Hakuna aliye salama. Haijalishi uzoefu wetu umekuwaje, haijalishi kituo chetu kiko juu kiasi gani, tunahitaji kukesha na kuomba daima. Ni lazima tutawaliwe, na kudhibitiwa kila siku na Roho wa MUNGU la sivyo tutatawaliwa na Shetani.

------------------------

Maswali: Barua hii aliandikiwa na nani? Kwa nini afya ya mwili na roho ni muhimu? Vitu kumi vya kusaidia afya zetu ni nini? Tofauti ya Diotrefe na Demetrio ni nini? Kwa nini ulafi ni jambo baya sana? Kwa nini ni muhimu kufuata mpango wa Mungu wa afya?

**SIKU YA 347.**
**(Desemba 12)**

**Waraka wa Yuda.**

# MUNGU anaweza kutulinda tusijikwae, tukimruhusu.



Barua hii ni ya waumini wote, na iliandikwa na ndugu ya Yesu, Yuda. Anasema anaandika kwa hao walioitwa na kupendwa na Mungu BABA. Hawa wamehifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo. Yeye aliandika awaonye watu na mafundisho ya uongo, yanayokuja. Anasema imemlazimu kuandika ili waishike sana imani waliyokabidhiwa, kwa maana kuna walaghai wanaojiingiza kwa siri. Hawa wameandikiwa tangu zamani kama makafiri na wanaobadili neema ya Mungu kuwa ufisadi na kumkana Mola na BWANA Yesu Kristo.

Anatukumbusha kwamba Mungu aliwatoa Waisraeli katika nchi ya Misri, ila wengi waliangamizwa njiani. Hawa walitendewa mema, bali wasiamini. Hivyo hata nasi leo tumemkubali Mungu na kumwamini. Twapasa tutembee Naye siku kwa siku. Tusichukue uzoefu wa jana wa kutembea na Mungu leo, la hasha, tutakuwa tunarudi nyuma hakika. Tusiangalie kama baba au mama walikuwa waumini bali sisi wenyewe tutatoa hesabu yetu binafsi hukumuni. Mungu hana wajukuu, bali wana tu. Tuwe kila siku tukimtafuta Mungu na kuenenda kutokana na Roho Mtakatifu.
Yuda anaonyesha kutii ni muhimu sana. Anatoa mfano wa malaika wa Mungu, ambao walishindwa kuilinda enzi yao. Hawa wamewekewa vifungo vya milele. Anatoa mifano mingi ya Agano la Kale mfano, Sodoma na Gomora kwa uasherati wakifuata dhambi wataadhibiwa. Kwa barua ya Yuda tunapata kuelewa kwamba

Musa alifufuliwa, na kwenda mbinguni. "Mikaeli Malaika mkuu alishindana na Ibilisi kuhusu mwili wa Musa, akimshitaki Musa kwamba ametenda dhambi, ila Mikaeli alisema, BWANA na akukemee."

Anazungumza njia ya Kaini mwuaji wa kwanza, na mwasi ambaye alipenda kujifanyia maagizo yake anayotaka, alipoambiwa kafara ya mpango wa Mungu ni mwanakondoo, yeye akaleta 'maharage mahindi, machungwa na matikiti' ikisimamia haki yake. Kumtii Mungu ni kufanya vitu kwa njia ile amepanga si kwa njia zetu. Alifikiri anamfanyia Mungu upendeleo/feva, akakataa kumwomba mdogo wake Habili kondoo. Mwanakondoo alimwakilisha Yesu aliyekufa msalabani. Bila kumwaga damu hakuna ondoleo la dhambi. Alipewa tahadhari kwamba dhambi inabisha mlangoni akadharau.

Watu wenye mafundisho yao wenyewe mbali na Mungu alivyoagiza, Yuda anasema ni kama mawingu yasiyo na maji au mvua. Ni miti iliyopukutisha maua, hivyo hukosa matunda. Miti iliyokufa mara mbili, yapasa kungolewa kabisa. Yuda anatukumbusha uasi wa Kora na Baalamu kwa kutaka njia zao, na mambo ya uongo, waliingia kwenye shida na kuwatia wengine kwenye shida. Watu wa namna hii wanaleta magomvi makanisani, na sehemu za ibada.

Yuda anatuambia Henoko aliyechukuliwa mbinguni bila kufa alipewa unabii wa kuja kwa Yesu kuchukua watakatifu akasema "BWANA aja na watakatifu Wake maelfu, maelfu, ili afanye hukumu na kutoa adhabu kwa wale wasiomcha." Kila mtu atalipwa kutokana na matendo au kazi zake. Anatuonya tusiwe watu wa kunung'unika na kulalamika kama Wanaisraeli miaka 40 jangwani. Mungu anachukizwa na malalamishi wakati anatusaidia katika yote, je kama mzazi unafurahi mtoto wako anapokulalamikia nawe umefanya jitihada zote kumpenda na kumsaidia? Wale Waisraeli waliingia mipaka ya Kanani mara tatu kabla ya kuvuka Kanani, na kurudi nyuma tena, kutokana na malalamiko.

Mara ya kwanza walituma wapelelezi Jeriko bali hawakuingia. Mara ya pili walifika Kadesh Barnea na kuumwa na nyoka, na kuangushwa na wanawake wa Midiani waliotumwa kama mitego ya Balaamu pia hawakuingia. Mara ya tatu ndiyo waliweza kuingia kwa kuvuka Yordani. Siku za mwisho watatokea watu wenye kudhihaki imani au Muumba, hasa katika wale wanaoona wamejiwezea na hawahitaji Mungu hata wakizufuata tamaa za upotevu. Hawa wasipoongozwa na Roho wa Mungu wanaleta utengano, maana hawaongozwi na Roho wa Mungu. Yuda anasema tujitenge na tuombe Roho Mtakatifu.

Tuhurumie wale wenye mashaka, na kuwaokoa kwa kuwanyakua kama vile tuonavyo mtoto asiyejua akiingia motoni, nasi tuwanyakue kutokana na uovu au kutomjua BWANA Yesu. Changamoto hii yatusaidia sisi tunaoishi mwisho wa historia ya dunia, tusiingie kwenye mafundisho ya uongo. Yuda anamaliza barua kwa kutupa moyo kwamba Mungu anaweza kutulinda tusijikwae na kutusimamisha mbele ya utukufu Wake bila mawaa katika furaha kuu. Yeye Mungu pekee, Mwokozi wetu katika Yesu Kristo BWANA wetu. Utukufu una Yeye na ukuu na uwezo, na nguvu hata milele. "Basi Kwake Yeye awezaye kutulinda tusijikwae na kutusimamisha mbele

ya utukufu Wake bila mawaa katika furaha kuu." Ni ahadi iliyoje! Je, tunaamini kweli kwamba Mungu anaweza kutupa ushindi juu ya kila dhambi inayotusumbua. Wengi wetu tunatatizika na kuwazia ubora huu wa hali ya juu. Tunatoa udhuru kushindwa kwetu kwa kulaumu urithi, asili ya ubinadamu, na kuchochewa lakini hatuna uhakika kwamba Mungu anakubali visingizio vyetu. Anatamani sana apate watu ambao kupitia kwao Yeye anaweza kuionyesha tabia Yake kwa ulimwengu, watu "ambao wangependa kufa kuliko kutenda tendo baya."

Ingawa ni kweli kwamba Bwana wetu Yesu anatufunika na vazi Lake la haki, hatuwezi kufanya hivyo huku tukiendelea kutenda dhambi inayojulikana wazi. Shetani angekuwa wa kwanza kupiga kelele, "Si haki Bwana! Ikiwa unaweza kuwafanyia udhuru hivyo, basi lazima unifanyie nami pia." Na angekuwa na hoja yenye mashiko. Ikiwa tunatoa udhuru kushindwa kwetu, na kushindwa kugeuka kutoka kwa makosa yetu katika nguvu za Kristo, basi dhabihu ya Kristo kwa ajili yetu ni bure. Tumeamua kwamba Yesu lazima atuokoe katika dhambi zetu, sio kutoka kwa dhambi zetu, ambalo ni tumaini la uwongo na lisilo na msaada wa kibiblia. Tunapojisalimisha kwa Yesu, tukimtazama Yeye kila mara kwa uongozi na nguvu, atatushika kwa mkono ambao hautauacha kamwe au kabisa (1 Kor.1:7-9).
Manabii wa uwongo, ambao kwa ajili ya pesa na sababu nyinginezo, wanawadanganya watu, hawataepuka uharibifu. Siku ya hukumu watasema, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kufanya maajabu mengi kwa jina lako? Ndipo Yesu atawaambia, "Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu! Mathayo 7:22-23 NKJV. Ili tusidanganywe nao, na kuangamizwa pamoja nao, tujifunze Biblia zetu ili kujua Ukweli.

*Omba Nyakati Zote—Jenga mazoea ya kuzungumza na Mwokozi unapokuwa peke yako, wakati unapotembea, na unaposhughulika na kazi zako za kila siku. Acha moyo uinuliwe kila wakati katika ombi la kimya la msaada, kwa ajili nuru, nguvu, na maarifa. Hebu kila pumzi unayovuta iwe sala.

-----------------------------------------------------

Maswali: Yuda anamwandikia nani hii barua? Henoka aliona nini kwenye maono? Kaini alifanya dhambi gani? Kulalamika na kunung'unika kuna shida gani? Mikaeli alishindana na Ibilisi kwa ajili ya nani? Yuda mwandishi wa waraka, ana uhusiano gani na Yesu?

**SIKU YA 348.**
**(Desemba 13)**

# UFUNUO. Upande wa Mungu unashinda, Haleluya! Mungu atahukumu na kuwazawadia watakatifu. Heri ya Asomaye.

**Ufunuo 1-2.**



"Nimesoma mwisho wa kitabu, nimeona upande wetu ndiyo umeshinda!" Imeimba kwaya moja ya injili maneno hayo. Kitabu cha Ufunuo ndicho cha mwisho kwenye Maandiko Matakatifu. Mtu aanzapo kusoma kitabu, hasa cha vita, matatizo yanayohitaji ufumbuzi au mafumbo yasiyo na majibu, anapenda kujua nani ni mshindi au kisa kitaishiaje? Sisi leo tumo vitani, mawazo yetu ni uwanja wa mapigano wenye makombora na mapigano mazito. Sisi tumechagua timu ya Mwenyezi Mungu aishiye mbinguni. Soma kitabu kipo mtandaoni, kinaitwa Pambano Kuu au The Great Controversy- Utajua ni jinsi gani vita tulivyonavyo ni vikali sana.
Baada ya kusoma sura tatu za kitabu cha kwanza cha Biblia (1,2 na 3) na Ufunuo 12. Utaona kwamba vita vilianza miaka 6,000 iliyopita. Kwenye kitabu cha Ufunuo sisi tulio upande wa Mungu ndiyo tutashinda. BWANA apewe sifa! Usipate jibu kwa maswali yako kwa wabashiri, wanajimu, wanasayansi, runinga, kompyuta, marafiki, wachawi au watu wa dunia, bali kwenye Biblia tu! Unabii wa Ufunuo au Apokalipsi ni kufunua Ahadi na upendo wa Mungu. Na si ujuzi wa kufunua matukio na mnyama! Tukiwa watu wa matukio na kusimulia mnyama kuliko ahadi na tabia ya Mungu tunapoteza dira. Unaposoma jihadhari usije ukakamata vitu vingine badala ya kuzishika ahadi za neema ya Mungu. Anasema uwe macho na kukesha kwa umilele maana Yeye Ajaye Yuko njiani! Unabii unamfunua Mungu.
Usipoteze muda wako kutafuta kubashiriwa nao, wewe kwa kutumia Biblia waweza kujua historia yote hadi mwisho. Utajua waovu na wale wa upande wa Ibilisi watakuwa kwenye timu ya upande usioshinda. Wao wenyewe wanaweza wasijue, ila wewe unajua. Kwa nini tusimwombe Mungu kila siku, atupe nguvu zote, kumimina

roho zetu kupata toba ya kweli, na kujiweka wakfu tukisoma Maandiko, ukisali, na kuwaambia wengine habari njema? Itakuwa vyema pia ujiunge na ushirika unaofuata mafundisho ya Maandiko kama yalivyo.
Kitabu cha Ufunuo kama jina lake lilivyo, kinaonyesha kimefunuliwa na ni kitabu kinachoeleweka. Twaweza tusijue yote maana sisi binadamu tunafunuliwa Neno la Mungu siku kwa siku, na hivyo hatuwezi kulijua lote kwa wakati mmoja. Hata mbinguni tutaendelea kujifunza milele zote. Ila Mungu ametufunulia kiasi cha kutosha kuweza kutupatia wokovu wetu. Narudia, kitabu cha Ufunuo si mafumbo au kificho tena. Wengi wanaokisoma kitabu hiki wanaona kimefunua yale nabii Daniel aliyoonyeshwa hapo zamani. Kitabu hiki kina mistari 407 ambayo kati ya hiyo 278 inatoka kwenye Agano la kale, hivyo Agano Jipya tu bila Agano la Kale haiwekani! Agano Jipya ni mwendelezo wa Agano la Kale, ni kama mtu kuwa na kiwiliwili bila kichwa. Mfano Farasi wane wanarudia katika kitabu cha Zekaria, na wale wanyama wane wenye sura za tai, Ng'ombe, Mwanadamu na tai wapo kwenye Ezekieli 1.
Danieli alipotaka kujua zaidi unabii aliopewa aliambiwa "Akasema, Enenda zako, Danieli; maana Maneno haya yamefungwa, na kutiwa muhuri, hata wakati wa mwisho." Kimefungwa mpaka wakati wa mwisho, na huu ni wakati wa mwisho. Karibu unabii wote umetimia. Uliobakia si ule utakaochukua muda mrefu. Tuombe Mungu atufunulie na chukua muda kukisoma kitabu hiki, maana kimefunuliwa tayari. Tunaishi wakati ule wa mwisho alioambiwa Danieli kwamba kitabu hiki kitaeleweka mno kuliko wakati Yohana na Danieli.
Yesu alimpa faraja na kumwambia Yohana atulie tu, asiwe na tashwishi kwani YEYE ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Aliyeko, aliyekuwako, na atakayekuwako. Alfa na Omega ni herufi ya kwanza na mwisho ya Kiyunani. Wayahudi walisema (Aleph na Taw). Mungu ni kila kitu hapungukiwi, Ni MWEZA. Yohana "mtume ambaye Yesu alimpenda" alipewa barua hii akiwa kizuizini kisiwa cha Patmo, kule Uturuki akiwa mzee wa karibia miaka 100 hivi! Kisiwa hiki kipo Uturuki kwenye bahari ya Aegen.
Miaka 60 hivi, ilikuwa imepita toka Yesu alipokufa na kufufuka, naye akajiuliza hivi mbona Yesu hajarudi mpaka leo? Aliwekwa kizuizini na Mtawala Domitiani wa Rumi. Yasemekana aliteswa mara nyingi, ila hakuuawa. Huu ulikuwa mwaka kama wa 90BK hivi. Yeye ndiye alikuwa mtume wa mwisho kufa. Yasemekana aliingizwa kwenye pipa la mafuta akaangwe, ila kwa muujiza hakufa. Alipenda sana kuzungumzia upendo.
Huyu 'mtume wa upendo' aliwaambia watoto na watu wazima "watoto wadogo pendaneni, maana tukipenda tumeitimiza sheria na tumevuka mauti na tumeelekea kwenye uzima." Soma tena 1 Korintho 13!. Yohana aliandika kwetu MUNGU NI UPENDO.
Kuharibiwa kwa Yerusalemu 70BK na Jemedari Tito kulikuwa kumeshatokea wakati huu na serikali ya Rumi ilikuwa imeanza kutesa watakatifu. Warumi waliendelea kuwatesa waumini hata mwaka 197 BK mkristo aitwaye Tertulo aliyewatetea Wakristo waliosingiziwa kuvunja sheria aliwaambia wahusika kwamba wale Wakristo waliotungiwa uongo ni tofauti ukilinganisha na wahalifu au wavunja sheria wengine. Waliteswa ili wakubali kwamba walitenda uovu, jambo ambalo halikuwa kweli na halikuwa halali.
Mateso haya yaliwaongezea ujasiri badala ya woga "Damu iliyomwagwa ya

Wakristo ikawa ni mbegu." Je, unachukua hatua gani mtu akikejeli imani yako? Unakata tamaa na kumkana Yesu, unalipuka na kurudisha makombora au unamkiri Mwenyezi Mungu?. Anaanza kitabu kwa kusema "Nalikuwa katika Roho siku ya BWANA nikasikia sauti nyuma yangu kama baragumu ikisema haya uyaonayo yaandike katika chuo, ukayapeleke katika makanisa saba ya Efeso, Smirna, Pergamo, Thiatira, Sardi, Filadelfia, na Laodikia.

Yohana akamwona Yesu katika utukufu Wake aking'aa na akiwa na vinara vile vya taa saba. Anaeleza alivyomwona, na sauti Yake kama sauti ya maji mengi. Yohana "alianguka miguuni pake akimsujudu, kwa hofu" ndipo Yesu akamwambia "Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho, na aliye hai, Nami nalikuwa nimekufa, na tazama ni hai hata milele na milele, Nami ninazo funguo za mauti na za kuzimu." Yohana mtume aliyekuwa mzee, na makunyazi ya uso, alijiona mpweke. Marafiki zake walikuwa wamelala usingizi wa mauti. Alikuwa akikumbuka mara nyingi miaka ile 31 au 32 aliyokaa na Yesu, na jinsi alivyobarikiwa na Upendo wa Yesu. Alikumbuka huduma ya upendo wa Yesu kwa maskini, watoto, yatima, wajane, na wote. Akakumbuka kifo cha Yesu na alivyoomba msamaha kwa wote, "BABA wasamehe maana hawajui walitendalo." Yohana akakumbuka Yesu alivyopaa. Sasa alikuwa anamwona Yesu tena! Hebu nasi tupate moyo kwamba tukiwa na huzuni Yesu Yupo na anatusikiliza shida zetu. Yesu hatasahau marafiki Zake, kama vile ambavyo hakumsahau Yohana.

Mungu atahukumu ulimwengu, na kuwapa thawabu watu waliomtumaini na kumtii katika maisha yao. Watu hawa wanaitwa watakatifu Wake Mungu Mwenyewe. Yesu Mwenyewe anafanya mpango ili Yohana apokee Ufunuo wa mambo ambayo hayana budi kuwako upesi. Yesu alipewa huu ujumbe na Mungu Baba Naye akatuma kwa mkono wa malaika, kisha malaika akamwonyesha mtumwa Wake Yohana, yale yanayokuja kutokea. Yeye asomaye na kusikia Maneno ya unabii huu wa Ufunuo na kuyashika yaliyooandikwa humu, ana heri maana wakati u karibu.

Zaidi ya mara nane Yohana anazungumzia kuhusu namba saba! Makanisa saba, mapigo saba, vinara saba, tarumbeta saba, mihuri saba, nyota saba, baragumu saba, joka mwenye vichwa saba, milima saba, wafalme saba, endelea kutafuta namba saba zingine. Mara nyingi Mungu anatumia saba kuwakilisha ukamilifu. Yesu akamwambia aandike yale ayaonayo ili ayasaidie makanisa yale atakayomweleza. Ndipo ayatume kwenye makanisa saba ya Asia ndogo kule Uturuki. Wanahistoria wengi wa kanisa kwa kuyaona yale yaliyoandikwa kwa makanisa yale, wameona yanawakilisha pia vipindi mbali mbali vya nyakati za kanisa la Kiristo.

Yesu anasema mazuri, mabaya, faraja, zawadi, changamoto, na kisha maonyo ya hilo kanisa ili lirudi kwenye utakatifu kama lina shida.

1. Kanisa la Efeso: Kipindi kinachowakilishwa 31-100BK.

Mazuri ni hawezi kuchukuliana na watu wabaya. Kanisa hili limejaribu mitume wa uongo, lina subira na uvumilivu kwa ajili ya jina la Mungu, na halichoki.

Mabaya: Wameacha upendo wao wa kwanza, wanayachukia matendo ya Wanikolai ambao walisema haijalishi matendo yako, ukimwamini Yesu inatosha.

Mashauri: Wakumbuke ni wapi walipoangukia wakatubu, warudie matendo ya mwanzo, yeye aliye na sikio asikie

Adhabu: Wasipotubu, nitakiondoa kinara chao.

Zawadi: Yeye ashindaye Yesu atampa kula matunda ya uzima.

*Njia ya kwenda kwenye kiti cha enzi cha MUNGU iko wazi kila wakati. Hauwezi kupiga magoti kila wakati kwa ajili ya maombi, lakini maombi yako ya kimya yanaweza kupaa kwa MUNGU kila wakati kwa ajili ya nguvu na mwongozo. Utakapojaribiwa, kama ambavyo huwa, unaweza kukimbilia mahali pa siri pa Aliye Juu. Mikono yake ya milele itakuwa chini yako.

---

Maswali: Yohana alikuwa kisiwa gani alipopata ndoto? Nani ni Alfa na Omega? Upande gani utashinda mwisho wa vita kati ya Mungu na Ibilisi? Kanisa la Efeso lilipewa mashauri gani? Je, tabia hizi za makanisa zinaweza kuwa kwenye kila nyakati?





**SIKU YA 349.**
**(Desemba 14)**

# Makanisa saba ya Asia Ndogo.

**Ufunuo 2-3**




2. Kanisa la Smirna: Kipindi kinachowakilishwa 100-331BK ambacho ni kipindi cha mateso.
Mazuri: U masikini kwa dhiki ila u tajiri kwa vile umenijua, unavumilia matukano na mateso
Faraja: Usiogope yatakayokupata, utatupwa gerezani na kujaribiwa na dhiki, "uwe mwaminifu hata kufa, Nami nitakupa taji ya uzima"
Onyo: Yeye mwenye sikio na asikie yale Roho iyaambiayo makanisa.
Zawadi: Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili.

3. Kanisa la Pergamo: Mwaka –Kipindi cha mwaka 331-538 BK.
Mazuri: Wakaa kwenye kiti cha enzi cha Shetani ila umelishika Jina Langu, wala hukuikana imani Yangu, hata Antipa shahidi wangu aliuwawa kwa ajili Yangu
Mabaya: Kuna watu wanaoshika mafundisho ya Balaamu yule aliyewafundisha kutia vikwazo kwa Israeli. Hawa wanatoa sadaka kwa sanamu, na hivyo kuwa na miungu mingine au hata kuzini. Kuna washikao mafundisho ya Wanikolai.
Onyo: Tubu, yeye aliye na sikio asikie, Roho aambiavyo makanisa.
Adhabu: Usipotubu nitafanya vita kwako na upanga.

Zawadi: Yeye ashindaye atakula mana iliyofichwa, atapewa jiwe Jeupe lililoandikwa jina Jipya asilolijua mtu ila Yeye.

4. Kanisa la Thiatira: 538-1500 BK
Mazuri: Ana matendo mazuri ya upendo na imani. Huduma za subira. Matendo yake ya mwisho ni mema hata zaidi ya mwanzo.
Mabaya: Wamuunga mkono na unamridhia au unamvumilia yule mwanamke Yezebeli mwenye mafundisho ya uongo, ajiitaye nabii, na kuwafundisha watumishi wa Mungu na kuwapoteza, ili wazini kwa kula vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu.
Adhabu: Nimempa Muda Yezebeli kuungama ila hataki, nitamtupa asipoungama, na kuua watoto wake. Nitamlipa kila mmoja kadiri ya matendo yake.
Onyo: Mlicho nacho kishikeni, hata nitakapokuja. Yeye aliye na sikio asikie.
Zawadi: Ashindaye nitampa mamlaka juu ya mataifa, atachunga na fimbo ya chuma. Nitampa nyota ya asubuhi

5. Kanisa la Sardi: Miaka 1,500-1,830 BK
Mazuri: Wako wachache sana wasiyotia mavazi yao uchafu. Wana mavazi meupe hawa wamestahili. Sitafuta majina yao kwenye kitabu cha uzima, bali nitayakiri mbele ya Baba Yangu na mbele ya malaika
Mabaya: Nayajua matendo yako una jina la kuwa hai nawe umekufa. Sikuona matendo yako kuwa yametimiliika mbele za Mungu.
Mashauri: Uwe mwenye kukesha ukayaimarishe yaliyosalia, yanayotaka kufa. Yashike Maneno ya Mungu uliyopokea na kusikia, na kutubu. Usipokesha naja kama mwizi, wala hutajua saa nitakayokuja. Yeye aliye na sikio alisikie Neno ambalo Roho ayaambia makanisa

6. Kanisa la Filadelfia: Miaka ya 1,830-1,840+
Mazuri: Una nguvu kidogo, nawe umelitunza Neno Langu wala hukulikana Jina Langu. Umelishika Neno Langu kwa subira Yangu
Zawadi: Nimekupa mlango uliofunguliwa mbele zako ambao hakuna awezaye kuufunga. Wale wa sinagogi la Shetani waovu watakuja kwako na kusujudu mbele ya miguu yako na kujua kwamba nimekupenda. Nitakulinda utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujia ulimwengu wote. Yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu. Nami nitaandika juu yake Jina la Mungu Wangu.
Mashauri: Naja upesi, shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako. Yeye aliye na sikio asikie Maneno haya ambayo Mungu anayaambia makanisa.
(Huu ni ule wakati watu wengi walifikiria kuwa Yesu atarudi, waliposoma Unabii wa Danieli 8:14, kumbe ilikuwa inahusiana na hukumu ya upelelezi)
7. Kanisa la Laodikia: Miaka 1,844 mpaka leo
Mabaya: Hu baridi wala mto, u vuguvugu, ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Wasema mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja na kitu, nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, mwenye mashaka, masikini, kipofu na uchi.' Ukimwona mtu asiye na nguo, mnyonge, mwenye mashaka na kipofu naye akakwambia kwamba hayupo uchi, na ni mwenye nguvu, na pia anaona vyema, utajua kwamba ana shida ya kichwa.
Adhabu: Kwa sababu hu baridi au moto, nitakutapika katika kinywa Changu
Mashauri: Inakupasa ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto. Upate

kuwa tajiri na mavazi meupe upate kuvaa. Aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya kujipaka macho yako, upate kuona. Wote niwapendao nawakemea na kuwarudi. Uwe na bidii ukatubu. Tazama nasimama mlangoni nabisha mtu akiisikia sauti Yangu na kufungua mlango nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami. Yeye aliye na sikio asikie Neno hili ambalo Roho wa Mungu ayaambia makanisa na watu binafsi.
Zawadi: Yeye ashindaye nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi kama Mimi nilivyoshinda, nikaketi na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi
Yesu anasema Yeye Yupo mlangoni anabisha, ili tumkaribishe. Je, upo tayari kumkaribisha Yesu awe Mwokozi, Mwalimu na Rafiki yako? Usimwache angoje nje bali mwambie "Yesu nina furaha kukukaribisha uishi moyoni mwangu milele!". Ila ni lazima uijue sauti Yake, maana hutafungua mlango kwa mtu usiyemjua, unaweza ukavamiwa na mtu mwingine! Kutapikwa ina maana kutolewa kwa msukumo wa nguvu toka tumboni na kutemwa nje umwagike huko kwa vile unaleta kichefuchefu. Mungu atusaidie tusiwe watu wa kumletea kichefuchefu!
Yohana alifikiri ni mzee na manufaa yake yameisha, kumbe alikuwa anaanza kazi kubwa kweli kweli! Ujumbe wa kitabu hiki ni kwamba Mungu Ndiye anayetawala wakati ujao. Tunapojaribu kudhibiti siku zijazo, tunafanya fujo. Shetani akitawala wakati ujao, atautumia kutuangamiza. Ikiwa majaliwa yangeamua wakati ujao, maisha hayangekuwa na maana. Lakini Ufunuo inafundisha kwamba wakati ujao uko mikononi mwa Yule anayetupenda na anayetutakia mema. Hii ni habari njema. Jinsi mambo yanavyoendelea katika ulimwengu wetu wa leo, mtu anaweza tu kutazama wakati ujao kwa hofu, lakini Ufunuo inatuambia kwamba Mungu ambaye anatupenda sana hata akajitoa dhabihu ili kutuokoa Ndiye mwenye mamlaka kamili. Haleluya!

Unabii wa Farasi wane, na Mihuri mine na Tarumbeta nne inahusiana sana na vipindi vya makanisa haya saba, hivyo ni marudio na ziada, ukitaka kujifunza zaidi waweza kuangalia notisi za Amazing facts au God cares (Daniel na Ufunuo) na Mervin Maxwell. Salvation in Symbols & Signs" by Ivor Myers and James Rafferty, na Gems of Revelation, and Gems of Daniel by Patrick Jones, na hata vitabu vya Kiswahili vya Daniel na Siku zetu, Ufunuo wa mambo yajayo. Ukiwa hauna hivi tuandikie barua, tulivyo navyo tutakutumia na kukuelekeza pa kupata vingine!

*Maombi ya Siri Yanafaa Pahali Popote, Wakati Wowote—Sali chumbani mwako, na unapoendelea na kazi yako ya kila siku acha moyo wako uinuliwe kwa MUNGU mara kwa mara.

----------------------------------------------

Maswali: Makanisa saba ya Ufunuo ni yapi? Kanisa la Sardi lina mema yapi? Kanisa la Thiatira lina mabaya gani? Kanisa la Filadelfia zawadi gani? Kanisa la Smirna linapewa maonyo gani? Kanisa la Laodikia lina shida gani? Je, twawezaje kuepuka kutapikwa na kuwa washindi? Je, twawezaje kuacha kujitegemea na shuguli zetu za kidini tunazofanya na kumtegemea Yesu? Je, umemkaribisha Yesu moyoni mwako leo alipobisha hodi? Swali la moyoni- Je, unaitambua sauti Yake kabla haujafunga mlango ili ujue si mwizi anataka kuingia?

SIKU YA 350.
(Desemba 15)

# Ni nani awezaye kukifungua kitabu?

**Ufunuo 5, 8-10**



Yohana alioneshwa enzi ya Mungu na kiti cha ufalme wa Mungu. Aliona mambo ya ajabu na mazuri. Wazee 24 pamoja na viumbe wane wa ajabu ambao kila mmoja alikuwa na sura yake. Wa kwanza, sura kama ya simba, wa pili, sura kama ya fahali, wa tatu sura kama ya mtu na wa nne sura kama ya tai. Hawa walikuwa na macho mengi mbele na nyuma wakijua yote yaliyokuwa yanaendelea wakimwakilisha Roho wa Mungu. Waliimba "MTAKATIFU, MTAKATIFU, MTAKATIFU."

Yohana akaangalia na kuona Mtukufu kwenye kiti cha enzi, ambaye kwenye mkono Wake wa kulia kulikuwa na kitabu kilichoandikwa ndani na nyuma, kimetiwa mihuri saba. Malaika akauliza "Ni nani aliyestahili kukifungua kitabu na kuvunja muhuri zake?" Wala hapakuwa na mtu mbinguni wala katika nchi wala popote aliyeweza kukifungua kile kitabu wala kukitazama.

Ndipo Yohana akalia kwa kuwa hapakuonekana mtu aliyestahili kufungua kitabu kile wala kukitazama. Ila mmoja wa wale wazee 24 akasema "Usilie, Tazama SIMBA aliye wa kabila la YUDA, shina la Daudi, Yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu na muhuri zake saba." Basi, Yeye yule Mwanakondoo aliyechinjwa ambaye ni YESU KRISTO akaja kukitwaa kitabu kile na wakaanguka wote wenye uhai kwa Mwana-Kondoo, na kila mmoja akiwa na kinubi, na maombi ya watakatifu wakaimba WIMBO mpya.

Wimbo ulisema "wastahili Wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake

kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa watu wa kila kabila, jamaa, lugha na mataifa." 10,000 x 10,000 x 1,000 walisema kama pambio tena (siku hizo namba zao zilifika elfu kumi tu!) "Astahili Mwana kondoo Aliyechinjwa kupokea uweza, utajiri, hekima, nguvu, heshima na utukufu", wakajibu "Amina" na wale wazee wakaanguka na kumsujudu Yesu (Waebrania siku hizo namba zao zilifika mpaka 10 elfu tu, hawakuwa na mamilioni, nasi kwetu hapa hazikufika hata elfu kwa lugha nyingi!. Wajua kwenye lugha zingine zilifika namba tatu tu yaani 1,2,3 na kisha wakasema ni nyingi tu!)

Zile muhuri zinapofunguliwa zinaleta shida, mateso na misukosuko mingi. Twaona farasi mweupe, mwekundu, kijivu na mweusi. Hatuambiwi kwamba Yohana alipewa maana ya farasi wale, ila kwa kuangalia historia, vilikuwa vipindi mbali mbali ambavyo kanisa lilipitia. Yawezekana zile rangi ni vipindi vile. Yule farasi mweupe, aliyempanda alikuwa Yesu Mwenyewe. Rangi nyeupe ilisimamia usafi, na ukamilifu wa kanisa katika upendo wake wa kwanza.

Hapa ndipo kanisa lilipoanza kuchukua ujumbe wakati wa himaya ile ya Warumi. Farasi mwekundu alisimamia kipindi cha mateso na wafia dini. Farasi mweusi alisimamia kipindi cha giza na mafundisho ya uongo, yenye udanganyifu unaopotosha. Farasi wa kijivu ni mchanganyiko wa mafundisho ya uongo na kweli. Anazungumzia baada ya hapo wanaonekana watu 144,000 waliopigwa muhuri, wenye mavazi meupe, naye anauliza ni nani hawa? (Rafiki yangu tunayeishi naye karibu sana kama maili kumi, aitwa Eric Garloff ana huduma inaitwa Sapphire throne na ana video za matukio yote haya, ya Ufunuo kurahisisha uelewaji, ya farasi hawa ilinivutia sana)

Akajibu hawa ni wale waliotoka katika dhiki kuu mwisho wa dunia, wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika Damu ya Mwanakondoo. Yaani wana tabia bora, isiyo na mawaa. Wamemkubali Yesu, wameungama dhambi zao, naye amewasafisha na kuwatakasa kwa neema Yake. Si kwamba wao ni wema kupita wengine, La! Bali wamekubali kumfuata Mwana-Kondoo kila aendapo, na kwa imani wamemtumaini Mungu na kumtii. Watu hawa wanamtumikia Mungu usiku na mchana katika hekalu lake na Yeye aketiye katika kiti cha enzi, ataandaa hema Yake juu yao "Hawataona njaa, tena wala kiu wala jua halitawapiga au baridi, maana Mwana-Kondoo atawachunga Naye atawaongoza kwenye chemchemi ya maji ya uhai yenye uzima. Na Mungu atafuta machozi katika macho yao yote. Je, nawe uko tayari kumfuata Mwana-Kondoo kila aendapo?

Anazungumza kuhusu baragumu saba zinazoonekana siku za mwisho wa dunia. Hebu tumwombe Mungu tusiwe kundi la wale waovu wafalme, wakuu wa dunia, majemedari, matajiri, watumwa na waungwana wale ambao "watajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, wakiiambia milima na miamba 'Tuangukieni, tusitirini, mbele ya Yeye aketiye katika kiti cha enzi na hasira ya Mwana-Kondoo'. Siku hiyo ya mwisho itakuwa ngumu. Ni nani kweli awezaye kusimama siku ile, ambaye hatakuwa na Vazi la Neema la Mungu au huruma na Neema za Mungu?

*Ilikuwa kwa njia hiyo ndiyo Henoka alitembea na MUNGU. Maombi haya ya kimya huinuka kama uvumba wa thamani mbele ya kiti cha neema. Shetani hawezi kumshinda yule ambaye moyo wake umejitegemeza kwa MUNGU.

---------------------------------------------------

Maswali: Ni nani aliyeweza kufungua kitabu na kuvunja mhuri wake? Kwa nini watu walijificha kwenye mapango na milima? Kwa nini wateule watakuwa tayari kumfuata Mwana-Kondoo kila aendapo? Tabia za watu 144,000 ni zipi?

**SIKU YA 351.**
**(Desemba 16)**

# Shetani alivyoanguka na malaika zake wakaja duniani.

**Ufunuo 12.**



Kulikuwa na vita na uasi mbinguni ambao tumeona kwenye kitabu hiki kwenye Mwanzo 3. Shetani alitupwa na theluthi moja ya malaika wote wa mbinguni. Akaja bustanini na kudanganya wazazi wetu wa kwanza, Hawa na Adamu. Shetani ni simba aungurumaye akitafuta ni nani amle, hivyo tuwe macho na kukesha kwa bidii, kwa kulisoma Neno la Mungu, tukisali na kuwaambia wengine, siku ya BWANA ya kuhukumu dunia inakaribia kwa upesi.

Watakatifu ndiyo watamhukumu Shetani na malaika zake. Hawa hawana furaha hata sasa, hata wao kwa wao wanagombana, wakimwambia mkuu wao 'Kwa nini ulitukosesha na kutufanya tutupwe toka mbinguni? Kwa nini ulitudanganya?' Shetani alipewa muda na malaika zake wa kutubu, ila kwa kiburi hakutaka kuacha hila zake mbaya. Hata leo tunapokosa tuungame mara moja ili tusije tukapotea siku

ya mwisho kwa kiburi na hata tuwapo duniani tukapigwapigwa na dunia. Moto na adhabu ya kifo cha milele ulitayarishiwa Shetani na malaika zake, na si binadamu. Joka kwenye Biblia ni jina la Shetani, au Ibilisi. Ibilisi ameshuka na ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache wa kudanganya watu. Anaitwa mshitaki wa ndugu, kwani anashitaki watu kwa Mungu kama alivyomfanyia Ayubu, akisema maovu ya watu, ila siku yake inakuja. Hebu Shetani anapokukumbusha mabaya uliyoyatenda, yaungame na kuwa na toba ya kweli. Kisha umkumbushe yale yanayomngoja kama adhabu yake hivi karibuni.

Wewe bado una nafasi leo, kumchangua Mungu, ila siku moja nafasi yako itaisha. Shetani hana nafasi tena. Alipewa muda, na mlango wake wa rehema ukafungwa, na siku yake ya kutubu ikaisha. Leo unaposikia sauti ya Mungu kumchagua, usiache Moyo wako kuwa mgumu. Mchague Mungu na Mwana-Kondoo wa Mungu aliyekufa kwa ajili yako. Isaya 12 na Ezekieli 28 yazungumzia zaidi kuhusu Shetani. Anaitwa mfalme wa Babeli au wa Tiro, ila ukiona zile tabia zinazotajwa unajua si za mtu bali ni za Ibilisi, aliyeumbwa kama nyota ya mwanga wa asubuhi "Lusifa." Alikuwa mkamilifu hadi dhambi ilivyoonekana ndani yake ya kujikuza, na uasi. Akitaka kuwa juu ya Mungu Mwenyewe, japo aliumbwa kama mwanadamu tu. Mungu aliweka malaika kuwa juu kidogo kwa mwanadamu bali si juu ya Mungu. Malaika hawapaswi kuabudiwa. Neno la Mungu laonyesha kila pale malaika alipopigiwa magoti na mtu alisema "inuka, mimi ni mjoli wako" Msujudie Mungu. Malaika waliumbwa, maana tunaambiwa "Katika Yeye vitu vyote viliumbwa vilivyo mbinguni, na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana, ikiwa ni vya enzi, usultani mamlaka na vitu vyote viliumbwa kwa njia Yake na kwa ajili Yake."
Hivyo malaika kama binadamu au viumbe vyote, wana mwanzo, ila Mungu hana mwanzo au mwisho. Mabilioni ya malaika wapo leo kwa ajili ya kushughulikia wokovu wetu, wao ni watumishi wa Mungu wakitusaidia kuhusu wokovu wetu na maslahi yetu. Eliya alipewa chakula na malaika na kupewa nguvu kihisia, kiroho na kimwili kuendelea mbele wakati mwanamke mbaya Yezebeli anamtafuta kumwua. Wengi siku hizi wamekuja na elimu isiyo ya Nuru ya Mungu kuhusu malaika. Na mara zingine hawatofautishi malaika wa Nuru na wa giza. Twapasa kujua malaika wapo na Biblia imelielezea hili vizuri, na ndilo Ukweli mtupu pekee. Neno linazungumzia malaika wa nuru na kazi zao zaidi ya mara 300. Mungu aliumba malaika na wapo, japo wachache wamejaliwa kuwaona, wote tumeokolewa kutoka katika shida kwa mpenyo, kwa sababu ya huduma ya malaika wa Mungu.

Malaika wametumika kutuokoa. Pengine nawe umesimuliwa jinsi watu walivyookoka au kusaidiwa kwa njia ya ajabu, na malaika waliowaona au wasiowaona. Wengine wamekutana na malaika kwa ajili ya kuwa na ukarimu kwa wageni, wamekaribisha malaika pasipo kujua. Ibrahimu baba yetu mwenye imani kuliko wote ni mfano wa waliokaribisha malaika bila kujua. Malaika hawaoi wala kuolewa. Malaika mbinguni hawatakuwa na uzoefu wetu. Twaambiwa kuna nyimbo au mambo wao hawatayaelewa vyema kama wanadamu maana wao hawakuokolewa na Kifo cha Yesu kama sisi. Malaika wana utashi mkubwa na uwezo wa mambo kuliko mwanadamu; ila hawana hekima, uwezo na maarifa kama Mungu, ndiyo maana Yesu alisema hawajui siku wala saa ya kuja kwa Yesu.

Malaika wanakula, tumeona kwa Ibrahimu alipowaalika, na hata tumeambiwa kwamba Waisraeli walikula mana, chakula ambacho ni cha malaika. Malaika tunaambiwa waliimba Bethlehemu Yesu alipozaliwa kuleta habari. Malaika walimhudumia Yesu baada ya majaribu, hata kwa ufufuo na kupaa juu watu waliona malaika hawa. Malaika wanamwabudu Mungu na Yesu kwenye kiti cha enzi, na furaha yao ni kuwa karibu na Mungu. Wanampenda ni ajabu; hasa walipoona matokeo ya malaika wenzao walivyoanguka, na jinsi Yesu alivyokuja na kufa kwa ajili yetu. Mashaka yao kwa upendo wa Mungu yaliisha kabisa Kalvari wakati Yesu alikufa, wakajua MUNGU NI UPENDO, na hili ni kweli tusiwe na mashaka nalo.
Kitabu cha Ufunuo kinaeleza kwamba kutakuwa na kupigwa muhuri kwa wale watakatifu. Wale ambao wameacha kuabudu mambo mengine ya duniani kama vile vitu, miungu ya kuchonga, mapokeo, na mambo ambayo ni kinyume cha ibada inayohitajika ambayo Mungu ameonyesha kwenye Neno Lake. Hawa watakuwa watu wanaoshika Amri zote za Mungu, na kuwa na Imani ya Yesu. Watakuwa na upendo wa Mungu. Malaika wanashangaa sisi wanyonge tusio na uwezo, tulivyo wavivu kumwomba Mungu, ambaye ana uwezo wa kutufanyia "mambo ya ajabu kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo."

Malaika wana ngazi, Mikaeli yupo juu. Pengine baada ya Lusifa kuanguka malaika Gabrieli alichukua nafasi Yake. Hili hatujui, ila twaona akitumwa kazi kubwa kubwa, kama kutangaza kuzaliwa kwa Yesu. Kuna aina mbili za malaika; Maserufi, na Makerubi. Maserufi wana mabawa sita, na makerubi mabawa manne, Soma Isaya sita na Ezekieli 10. Ili usiingie kuabudu au kuwafuata malaika wa Mwovu jua tofauti kati ya malaika wa nuru na wa giza. Kimbilio letu ni Neno la Mungu, hili ndilo litupatialo uwezo wa kuwatofautisha. Si miujiza au ishara kwanza, ila Neno la Mungu kwanza, kisha ishara na miujiza.

Mungu ametupa tahadhari ya malaika wa giza na kazi zao, zile za matunda ya mwili ya uovu ya Wagalatia. Japo Isaya 13 yasema kwamba Shetani afanya kazi kuangusha mataifa, na jamii, akitingisha ufalme wa Mungu kwa kutumia majanga, dhiki, uongo, na uerevu, Yesu ni mshindi. Siku moja Shetani atahukumiwa na kuangamizwa kwa maana "mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele."
Ila Neno la Mungu lasema "Wakamshinda Shetani na damu ya Mwana-kondoo, yaani Yesu Kristo." Watu wanaompenda Mungu au Yesu Kristo, hawajipendi maisha yao kwanza, ila Mungu kwanza nao wako tayari kufa kama ni mapenzi ya Mungu. Wokovu nguvu, ufalme na mamlaka ni kwa Mungu.

Vita ni kitu kibaya sana. Na vita daima hutokea kwaajili ya ubinafsi. Kumekuwa na maelfu ya vita baada ya vita hivi vya mbinguni. Je, unajua vita vikuu vya pili vilitokeaje? Ilikuwa ni kwaajili ya ubabe wa Ujerumani chini ya kiongozi wao Hitler alipoivamia poland mwaka 1939. Jambo hili likasababisha ufaransa na uingereza kutangaza vita kwa ujerumani, na wakapata msaada wa nchi zingine kama Marekani, wakapigana miaka sita, na mwishowe walipoona wanaenda kushindwa na ujerumani iliyokuwa imejiunga na wajapani na waitaliano, walitupa bomu kule japani Hiroshima, na hivyo upande huo wa ujerumani ukasalimu amri, yasemekana watu zaidi ya milioni 60 walikufa, hii ni kama idadi ya watu wote wa nchi ya Tanzania

leo! Yote ni kwasababu ya ubabe, ubinafsi, na kukosa upendo wa binadamu ambaye aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Biblia yasema kamwe hatutajifunza vita tena mbinguni! Leo tumeona mapigano ya vita kule Kongo, Korea, Somalia, Sudani, Ethiopia na Ukraine yanavyosababisha huzuni nyingi. Tuzidi kuombeana na kuwakumbuka wale walio vitani, ambao wengi wao hawapendi kuwa na vita, ila ubinafsi wa watu wachache umepelekea jambo hilo kutokea.

*Hakuna wakati au mahali ambapo hapafai kutoa ombi kwa MUNGU. Hakuna kitu kinachoweza kutuzuia kuinua mioyo yetu katika roho ya maombi ya bidii na unyofu. Katika umati wa watu waliosongamana mitaani, katikati shuguli za biashara, tunaweza kutuma ombi kwa MUNGU na kuomba mwongozo wa MUNGU, kama vile Nehemia alipofanya ombi lake mbele ya Mfalme Artashasta. Ushirika wa karibu unaweza kupatikana popote tulipo. Tunapaswa kuacha mlango wa moyo wazi daima na mwaliko wetu ukienda juu ili Yesu aje na kukaa kama mgeni wa mbinguni katika nafsi.


-------------------------------------------------

Maswali: Kuna tofauti gani kati ya maserafi na makerubi? Malaika wana kazi gani? Je, mafundisho gani ni ya uongo kuhusu malaika? Joka ni nani? Kwa nini ni dhambi kuabudu malaika?

**SIKU YA 352.**
**(Desemba 17)**

# Mnyama wa kwanza na wa Pili.

**Ufunuo 13.**



Hapa anazungumza kuhusu wanyama wawili. Wa kwanza akitoka baharini mwenye pembe kumi na juu ya kichwa chake vilemba kumi, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru. Mfano wake ni chui, miguu kama dubu, na kinywa kama simba. Ana nguvu za joka yaani Shetani, amempa uwezo mwingi. Watu walimsujudu joka kwa sababu alimpa uwezo huyo mnyama. Pembe yaonyesha ni falme. Yasema falme hii itafunua kinywa imtukane Mungu kwa maneno ya makufuru, na kufanya vita na watakatifu wa Mungu. Bahari kwenye unabii humaanisha pahali penye watu wengi. Utawala huu unahusiana na ule wa Daniel 7 ambao ni ufalme wa Rumi.

Kila ambaye hakuandikwa jina lake kwenye kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo atamsujudu yule mnyama. Anasema hii himaya ya kwanza ilitesa watu kwa miaka 1,260 au miezi 42 x 30 = 1260. Biblia inasema, "akapewa kufanya vita na watakatifu" kisha yasema "watamsujudia kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia. Mtu akiwa na sikio asikie."Yaani Mungu atawapa watu hekima kupambanua ili wasimsujudu mwingine isipokuwa Yeye. Hatuwezi kutumikia mabwana wawili. Kwa njia ya maneno, mawazo, matendo na nia zetu kila siku tunamtumkiia Mungu au Ibilisi.

Jiulize leo, Je, unataka kumtumika nani? Mnyama wa kwanza aliyetoka baharini, nayo mara nyingi yamaanisha atoka walipo watu wengi, wa pili atoka nchi kavu akimaanisha alitoka kwenye watu wachache. Mnyama wa pili pia ni falme au mamlaka atakayenena kama Joka au Shetani, na kutumia uwezo wa mnyama wa kwanza, akifanya dunia yote na wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza. Akawakosesha wakaao juu ya nchi. Akafanya watu wadogo na wakubwa, matajiri na masikini na walio huru kwa watumwa wapate chapa mkono wao wa

kuume. Zile pembe mbili zilionyesha utawala wa aina mbili, wa serikali na wa kanisa ukiwa umetofautishwa kwanza. Wanahistoria wanaona ufalme huu jinsi ulivyoibuka na kuendelea unafanana na Nchi ya Marekani.

Wakati huo watu hawataweza kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile au hesabu ya jina lake, na hesabu yenyewe ni ya kibinadamu, yaani namba 666. Hili ni jambo la kumwomba Mungu ili sisi watoto Wake atueleweshe. Wengi wamesema ufalme au kiongozi huyu ni mpinga Kristo. Kutokana na maelezo ni kweli tabia yake yaonyesha anampinga Kristo. Sisi tusiwe na hofu ya hilo, bali tudumu tukisali na kuomba Mungu atusaidie wakati wa mwisho na wa hatari, maana YEYE Ndiye mshindi hatimaye. Unabii mwingine tunapewa ili ukitokea tujue kwamba Yeye ni wa Kweli. Kabla haujatokea hatuwezi kuelewa au kuwa wazi. Pia unapotokea hatuwezi kujua kinachoendelea, ila ukimalizika tutaelewa vizuri.

Mfano ni unabii wa kuzaliwa kwa Yesu, wengi hawakujua, walifikiri Yesu amekuja kuleta ufalme Wake baada ya kuzaliwa, wasijue kwa hakika kwamba atateswa, atauwawa na kufufuka. Ila leo tukisoma Neno Lake tuna baraka na bahati mno kwamba tunajua kilichokuwa kinaendelea. Mitume hawakujua yale tunayojua leo. Siku zile hata Neno la Mungu lilikuwa halijaanza kuchapishwa, watu walilinakili kwa masaa mengi. Ila siku hizi, kila mmoja akitaka aweza kuwa nalo. Hebu omba Mungu akusaidie ununue Biblia na kuisoma Kila siku. Rudi kwenye madhabahu, asubuhi na jioni, maana ni 40% tu ya waumini ambayo huomba asubuhi na jioni, nasi yabidi tuombe kwa kusihi, ili Mungu aongeze jeshi ya watu wa maombezi. Kimbilio Letu ni Neno la Mungu na Mungu Mwenyewe na si maneno ya matisho.
Haitatusaidia tukijua kwa undani kila unabii na tusitende. Kutii sauti ya Mungu na kubadilika ndiyo muhimu na kipaumbele. Mungu anatufunulia kidogo tu, yale ambayo tukijua yatatusaidia, ili tusichanganyikiwe. Jambo kubwa ni kujiuliza "Je mimi ni mpinga Kristo?" Maana Biblia yasema kwenye kitabu cha Wathesaloniki na hii Ufunuo 13 kwamba mpinga Kristo atakuja, au ameshakuja na yupo sasa hivi ila unaweza usimfahamu huyu ni nani. Je, mimi ni mpinga Kristo? Nimejiuliza. Je, wewe ni mpinga Kristo? Kila mtu ana tabia hii ya kumpinga Kristo, kwa mawazo, maneno, matendo, na hata nia. Ila yule atakayeharibu mambo zaidi, atakuwa mtu aliye kanisani na mwenye mvuto wa kiutawala duniani, huyo atawadanganya wengi hakika.

Leo jiulize, Je, nina vitabia vya kumpinga Kristo? Ni vipi ivyo ili niviondoe? Mungu harekodi mawazo, maneno au matendo yetu tu bali hata nia ya mioyo, mitazamo au hata shauku zetu. Kuna siku tutasimama hukumuni na kutoa hesabu ya kila jambo, hapo ndiyo mwisho wa kila mtu utakapoamuliwa.

*Maombi Yanatuleta Katika Uwepo wa MUNGU Mwenyewe—Maombi , iwe yanatolewa katika mkusanyiko wa watu wote, kwenye madhabahu ya familia, au kwa siri, humweka mwanadamu moja kwa moja mbele za MUNGU. Kwa maombi ya kudumu vijana wanaweza kupata kanuni zilizo imara sana kiasi kwamba majaribu yenye nguvu zaidi hayatawavuta kutoka katika uaminifu wao kwa MUNGU.
--------------------------

Maswali: Soma Ufunuo 13 uwaelezee wanyama hawa wawili. Utajuaje kama wewe au mtu Fulani ni mpinga Kristo? Mtu hataweza kununua au kuuza isipokuwa ana chapa, au hesabu ile, ni namba ngapi hiyo? miaka mingapi au miezi mnyama alipewa kufanya vita na watakatifu? Taja sababu unabii umepewa kwetu. Mwelezee mnyama wa kwanza, Mwelezee mnyama wa pili? Mpinga Kristo ni nani? Mnyama aliyetoka baharini na aliyetoka nchi kavu wana tofauti gani?

**SIKU YA 353.**
**(Desemba 18)**

# Malaika wanne na watakatifu 144,000.

**Ufunuo 14-17.**



Yohana akaonyeshwa tena wale watu 144,000, wenye Jina la Mungu kwenye vipaji vya nyuso, wakipiga vinubi na kuimba wimbo mpya ambao watu hawa 144,000 tu ndiyo waliujua. Hawa 144,000 walikuwa wale walioishi bila mawaa, watakatifu na waaminifu, na walikuwa wanamfuata Mwana-Kondoo kila aendapo. Hawa ni wanadamu walionunuliwa, na ni malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo. Vinywa vyao havikuonekana na hila au uongo, maana hawakuwa na mawaa. Yaonekana, hawa ndiyo wale waaminifu waliokutwa bado wanaishi wakati wa Yesu kurudi, ambao hawataonja mauti.

Kisha Yohana akaona malaika akiruka mbinguni mwenye injili ya milele ambaye anaelezea ibada ya Kweli ile ambayo Mungu anataka. Huyu aliwahubiri watu wakaao juu ya nchi, na kila taifa kabila na lugha na jamaa akisema kwa sauti kuu "Mcheni Mungu na kumtukuza kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja. Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Kisha

akaja malaika wa pili akitoa onyo kuhusu ibada ya uongo akisema “umeanguka umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa maana ndiyo uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake.”

Na malaika wa tatu anayetangaza adhabu kwaajili ya ibada ya uongo akaja na kusema “Mtu yoyote atakayemsujudu mnyama wa Ufunuo 13 na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa pasipo kuchanganya maji, katika kikombe cha hasira Yake, naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele ya Mwanakondoo.” Akatangaza kuwa hiyo ndiyo itakayokuwa adhabu kwa wote wamsujudiao mnyama na sanamu yake, na kupokea chapa yake. Hapo ndipo penye subira ya watakatifu hao wazishikao Amri Zake Mungu na imani ya Yesu. Akasema heri wafu wafao katika BWANA japo wapate mateso, watapumzika baada ya taabu zao, kwa kuwa matendo yao mazuri yawafuata.

Kisha akaona Mwana wa Adamu yaani Yesu, akiwa tayari kuvuna wateule maana mavuno yamekomaa. Uvunaji kwa uzima wa milele ukaendelea. Kisha akaona malaika wanne, wakivuna. Hawa wanawakilisha pande nne za dunia, kusini, kaskazini, mashariki na magharibi. Anaendelea kuelezea habari za malaika saba wenye mapigo saba ya mwisho wakitokezea na kuvimimina vitasa vya majanga makubwa. Tumwombe Mungu na tuwe upande Wake, ili tusipate mapigo haya, maana hata Misri wale waliomtumaini Mungu waliepuka mapigo saba yale mabaya ya mwisho.

Tunaona yule wa saba alipomimina kitasa sauti ikatoka kama siku Yesu alivyokufa msalabani “Imekwisha”, pakawa na umeme na radi kubwa. Kila kisiwa kikakimbia, wala milima haikuonekana. Mvua ya mawe ikashuka, na waovu wakapigwa na mawe hayo, wakamtukana Mungu kwa vile pigo lile lilikuwa kubwa mno. Basi sisi tujiweke kwenye kumtii Mungu na kusoma Neno Lake ili tusiwe wale tunaomtukana Mungu bali kumsifu, kumshukuru na kutumtukuza tukisema “makuu ni matendo yako, umetutoa mbali na kutuokoa, na shida na hasira zote”

Yohana akaonyeshwa mwanamke kahaba, ameketi juu mnyama mwekundu sana, alikuwa na kikombe cha dhahabu kilichojaa machukizo kwa Mungu, na kwenye kipaji cha uso wake iliandikwa “Babeli mkuu, mama wa makahaba na machukizo ya nchi.” Mwanamke huyu alilewa damu ya watakatifu. Kuwa kahaba kwenye Neno la Mungu ni kuwa na mafundisho ya uongo. Na kulewa damu ya watakatifu, maana yake ni kutesa watakatifu, au wafia dini. Wale watu ambao wako upande wa kahaba au mafundisho ya uongo tunaambiwa majina yao hayajaandikwa katika kitabu cha uzima.

Yesu amemshinda Shetani. Ili kushiriki katika ushindi Wake dhidi ya Shetani, ni lazima tujitolee Kwake kama vijana watatu wa Kiebrania, Shadraka, Meshaki na Abednego walivyokuwa (Danieli 3). Kwa maneno mengine, kujitolea kwetu kikamilifu kwa Yesu, na uaminifu katika kuhubiri injili, hutuhakikishia kushiriki ushindi Wake dhidi ya Shetani. Yaani ushindi huu uwe wetu!

Pembe inasimamia falme, ambapo hapa zinampa
nguvu yule mnyama na mamlaka yake. Mnyama huyu atafanya vita na Mwana-Kondoo, ila atashindwa kwani Mwana-Kondoo ni BWANA WA MABWANA NA MFALME WA WAFALME. Baadaye wote wataangamizwa.


*Katika ibada ya siri maombi yetu hayatakiwi kufikia masikio ya yeyote ila MUNGU asikiaye maombi. Hakuna sikio lenye udadisi linalopaswa kupokea mzigo wa maombi hayo
---------------------

Maswali: Kwa nini tumche Mungu na kumtukuza? Mwanamke kahaba ni mwovu kwa sababu zipi? Sema kile walichokisema malaika watatu? Je, ni mabadiliko gani unayoyaona duniani leo yanayokuonyesha kuja kwa BWANA ni karibu?

SIKU YA 354.
(Desemba 19)

# Kuepuka mafundisho ya uongo.

**Ufunuo 18-20.**



Yohana akaona malaika akishuka kutoka mbinguni mwenye mamlaka kuu na dunia ikaangazwa na utukufu Wake. Akasema "Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza." Akasikia sauti watu watoke kwake Babeli wasishiriki dhambi yake maana dhambi zake zimefika mbinguni. Babeli huwa inawakilisha mafundisho maovu, ya ulaghai, kando kabisa na yale ya Biblia Mungu aliyotupa. Babeli pia inawakilisha machafuko yahusuyo uovu kama yale yaliyotokea kwenye mnara wa Babeli wakati lugha tofauti zilipoanza na watu wakatawanyika.

Japo hatujui tafsiri ya baadhi ya Maandiko katika kitabu cha Ufunuo kama watoto wa Mungu, tukazie kuepuka mafundisho ya uongo yasiyo kwenye Biblia. Kama mafundisho hayapo kwenye Biblia tusiyafuate. Biblia yapaswa kujitafsiri yenyewe. Nasi twapaswa kuomba kabla ya kuanza kuisoma. Mapokeo ya kibinadamu yapasa tuyaepuke. Biblia ikisema, tufuate jambo, basi hilo ndilo tunapaswa kuangalia. Tuisome, tuikariri, tuithamini, tuitafakari, tuiamini, na tuitii kwa vitendo. Yaonekana kitabu hiki kinazungumzia hukumu, kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Yohana a sema "furahini juu Yake enyi mbingu, nanyi watakatifu, na mitume na manabii, kwa maana Mungu amehukumu hukumu yenu juu yake.
Kwa mtu anayempenda Mungu, hukumu ni jambo zuri, na si jambo la huzuni, maana

Mungu anamfunika na Neema Yake. Yupo upande wa Mungu, akimtii MUNGU na kumwamini, Yuko upande wa ushindi. Ameshafunga goli. Yohana anaona makutano mengi mbinguni, ya viumbe wa MUNGU wakisema Haleluya, wokovu na utukufu, na nguvu zina BWANA wetu kwa kuwa hukumu Zake ni za haki na kweli. Hapa MUNGU atakuwa amehukumu wote waovu, kama yule kahaba, na zile falme zenye uovu. Wazee 24 wakasujudu na wenye uhai nao wakamwabudu MUNGU na kumsifu wadogo kwa wakubwa. Watu wakafurahi nao wakaimba "Haleluya Mwenyezi amemiliki, na tufurahi na kushangilia na kumpa MUNGU utukufu."

Watu wema wana mavazi ya kitani, ambayo ni matendo ya haki naye akaambiwa "Heri walioalikwa karamu ya arusi ya Mwanakondoo." Mimi na wewe tumealikwa pia, MUNGU Ashukuriwe. Tunaambiwa hapa YESU ana Jina limeandikwa kwenye vazi na paja Lake "MFALME WA wafalme na BWANA wa mabwana." Majemedari wa uovu na watu hodari, watumwa na waungwana wadogo na wakubwa wote walipata adhabu. Wale ambao hawakutaka kumfuata MUNGU tunaona myama, anakamatwa na manabii wa uongo waliosemwa. Wale wote waliodanganya watu kupokea chapa na kusujudu kwa wengine ambao si MUNGU.

Malaika akashuka toka kuzimu na kumfunga Ibilisi, yule Joka wa zamani, aitwaye Shetani akafungwa miaka elfu. Kufunga hapa yaweza kumaanisha mazingira ya kumfunga ili asipate kumdanganya mtu tena. Yohana akaona viti vya enzi na wale watu walikufa kwa ajili ya ushuhuda wa YESU na kwa ajili ya Neno la MUNGU wakafufuliwa na kuwa hai. Huo ndiyo ufufuo wa kwanza, wa wenye haki. Ufufuo wa kwanza ndiyo ule wa baraka na heri, wa watakatifu. Hawa hawatakufa mauti ya pili ya milele. Mauti ya kwanza ni hii tunayoijua tunayokufa duniani leo. Mauti ya pili ni ile ya kuangamia milele, au kutokwenda mbinguni. YESU alikufa mauti ya kwanza na ya Pili ili aweze kutuokoa kutoka katika adhabu na janga hilo la mauti ya pili ambayo ni mauti ya milele.

Itakapokwisha miaka elfu, Shetani atakapofunguliwa atataka adanganye watu tena. Atataka afanye vita tena na watakatifu na mji wa MUNGU wa Yerusalemu mpya unaoshuka. Atajaribu kuleta mabaya kwa mara ya mwisho tena, na kuzingira kambi ya watakatifu na mji huo wa Yerusalemu uliopendwa. Ila moto utashuka toka mbinguni na kuwala, na Ibilisi atakuwa katika ziwa la moto, na kiberti na huyo mnyama na nabii wa uongo watateketezwa.

Yohana akasema, aliwaona wafu wakubwa na wadogo wamesimama mbele ya kiti cha enzi na vitabu vikafunguliwa. Kitabu cha uzima kikatumika kuhukumu wote. Matendo yetu yote yanaandikwa, hakuna la kufichwa. Kila nia, wazo, neno, shauku, hisia na tendo liko wazi mbele ya MUNGU. Tukiungama mabaya yetu yanafutwa, maana MUNGU ana MFUTO mkubwa kupitia kwa Damu ya YESU. Bahari ikatoa wafu waliokufa, na nchi ikahukumiwa kwa matendo yao. Mauti na kuzimu vikatupwa maana wote tutaishi milele, tuliomchagua MUNGU. Ila mtu asiyeonekana kwenye kitabu cha uzima atatupwa kwenye ziwa la Moto.

Ombi letu ni MUNGU atusaidie tujitoe kikamilifu Kwake, na kuishi kwa mpango wa MUNGU ili tuwe mbinguni. Ushauri kwa uimbaji wetu tunapojizoesha hapa duniani!

Muhimu kuzingatiwa katika huduma ya Muziki ili muziki wetu uwe na kicho

1. Muziki wa waumini ni muhimu uonyeshe heshima na kicho kwenye ibada kwani ndio wakati tunakutana na Mungu, Na pia uendane na Maandiko matakatifu, na si kutunga vitu vinavyokiuka Maandiko.
2. Vyombo vya Muziki vichezwe kwa upatanifu na visisikike zaidi na kuzuia maneno ambayo ndiyo yamebeba ujumbe wa Mungu.
3. Muziki unapotolewa uonyeshe Furaha na uchangamfu wa kuwa mbele za Mungu (Uf. 7:12)
4. Uwiano uwepo katika Ujumbe unaotolewa na mpangano wa Sauti na ulete somo mahususi linaloweza kueleweka
5. Waimbaji wa Kwaya ya Kanisa na Vikundi wawe na sare kadri iwezekanavyo au mavazi ya heshima ya kujiwasilisha vizuri mbele ya watu na Mbele za Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana.
6. Muziki na huduma ya Uimbaji katika maandiko ni sawa kama Sadaka ya Shukrani kwa Mungu, Ya Uumbaji, ulinzi wa Mungu na Wokovu wa Milele. Angalia kwaya ya watu 4000 ilivyokuwa inafanya kazi kama Watumishi wa BWANA.
7. Hebu tufanye matengenezo ya kuturejesha katika mapito ya zamani wa Muziki wa Kiadiventista. (Yeremia 6:16.) Mungu na awabariki.
MUNGU AWE NASI.

*Maombi ya faragha yanapaswa kuwa ya Siri — Katika maombi ya faragha wote wana nafasi ya kuomba maadamu wanamatamanio ya kufanya hivyo na kujieleza kinagaubaga kwa Mungu kama watakavyo. Wanaweza kuwaombea ndugu na marafiki zao wote. Chumbani mwako, pale mahali pa faragha, ni mahali pa kusema shida zako zote binafsi, na mitihani, na majaribu. Mkutano wa pamoja wa kumwabudu Mungu si mahali pa kufungua mambo yetu binafsi ya moyoni.
--------------------------------

MUNGU: Kuna tofauti gani kati ya mauti ya kwanza na ya pili? Shetani na wafuasi wake watataka wafanye nini baada ya miaka elfu? Mauti na kuzimu vikatupwa ina maana gani? Babeli ina maana gani? Kitabu cha uzima kina nini? Vazi la kitani ni lipi? Kwa nini tufuate Neno la MUNGU na si mapokeo ya binadamu?

**SIKU YA 355.**
**(Desemba 20)**

# Jehanamu I



MUNGU ana njia nyingi za kutusaidia kwa kutuwekea vizuizi au wigo ili tuokoke. Yawezekana Jehanamu ikawa kizuizi cha mwisho cha kutusaidia tuokoke. Mara nyingi watu wamesoma na kuzungumzia kuhusu Jehanamu. Watu wamekuwa na mafikira mbali mbali kuhusu mahali hapa. Wengine wamekuwa na picha vichwani mwao jinsi Jehanamu ilivyo, bila ya kuangalia Maandiko yanasemaje. Je, waweza kueleza Jehanamu unavyoifahamu? Je, Maandiko Matakatifu yanasema nini kuhusu Jehanamu? Je, Maandiko Matakatifu yanataka tujue kuhusu Jehanamu? Na kama yanataka tujue kuhusu Jehanamu, yanataka tujue yapi, na kwanini tujue hayo? Hatuwezi kuandika Visa vya Biblia kwa 'wadogo' bila kuzungumzia mada hii, kwa kuwa ni ya muhimu. Hii ni kwa vile kuna mwisho wa safari yetu, baada ya hukumu. Kuna mahali pawili tu; mbingu na jehanamu. Upendo wa MUNGU umezungumziwa zaidi ya mara elfu moja kwenye Maandiko, na wengi husoma na kuishia pale. Lakini ghadhabu ya Mungu imetajwa katika Biblia mara 584. Hasira ya Mwana-Kondoo ya Ufunuo sita inatutatanisha kwani tumezoea Mwana-Kondoo akiwa mtoto wa kondoo mpole. Lakini tufahamu pia kwamba Mwana-Kondoo ni Simba wa Yuda. MUNGU ni upendo ila anachukia dhambi, kwa kuwa inaharibu maisha na furaha ya viumbe Vyake kwa njia ya mauaji, ujambazi, uasherati, magonjwa, vita vya makabila, au ubakaji.

Kama Biblia imetuandikia kuhusu kwenda mbinguni, tukichagua kwenda, basi kuna haja ya kuzungumzia kwenda motoni au Jehanamu. Kuna uchaguzi wa aina mbili, au falme mbili tu. Mbingu na Jehanamu, ni mambo ya uhakika kabisa. Siku ya leo, tutaangalia mafungu machache tu yahusuyo jehanamu au adhabu za waovu. Ama kwa lugha nyingine ni kwamba mwanadamu amepewa fursa ya kufanya uchaguzi katika maisha yake, naye amewekewa vitu viwili: uzima na mauti. Yule anayechagua uzima maana yake amechagua paradiso (peponi) au mbingu na yule anayechagua Jehanamu maana yake amechagua moto au kupotea milele. Kila mmoja anaweza kuchagua upande anaotaka kwa sababu Mungu hamlazimishi kiumbe Chake kufanya mambo kwa lazima. Yeye hakuumba roboti watakaompenda na kumtumikia bila utashi. Ametupa sote uchaguzi, ambayo ni hatari kwetu kwani tunaweza tumfuate au tumwache! Ila tunapotumia uchaguzi au uhuru wetu vyema tunakua kiroho na upendo wetu unakuwa wa kweli na unaendelea kuwa mkubwa! Yaani siyo feki! Au Bandia!

Wengi wamesoma kuhusu ghadhabu ya MUNGU wakaogopa. Kuogopa kuna uzuri wake pia, kunatusaidia tuweke mambo sawa. Cha kukumbuka zaidi kuhusu Jehanamu, ni kwamba Jehanamu au adhabu hiyo haikuwekewa binadamu. Ni Shetani na malaika zake tu, ambao walipewa muda kuungama bali hawakutaka kufanya hivyo, hao ndiyo waliotayarishiwa Jehanamu. Jehanamu si moto wa milele au adhabu ya milele, kwani Mungu hakuahidi uzima wa milele kwa waovu. MUNGU alimtoa Mwanawe wa pekee, kuwa kafara ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele (Yohana 3:16).

Wengi wamesema kwamba MUNGU ni moto ulao. Wale wote wenye dhambi atakapojaribu kuwakumbatia kwa upendo, watakuwa na maumivu yanayowachoma maana Mungu ni moto ulao dhambi, ila akiwakumbatia wenye haki, kwao litakuwa kumbatio la furaha na upendo. Bila shaka kule mbinguni hakuna hata mmoja atakayetaka kuishi na mtu asiyebadilika tabia. Kila mtoto au mzee amechoshwa na tabia hizi mbovu za hapa duniani, na hana hamu ya kuzikuta kule mbinguni tena, la sivyo haitakuwa mbingu! Ukikaa na jirani yako mbinguni na aje kukuibia vitu vyako, au kukupiga wakati umebarizi raha mstarehe, basi hautakuwa mbinguni, utakuwa kwingine. Je, MUNGU afanyeje basi, ili tabia hizi mbaya za ubinafsi ziishe ili kila mtu aishi raha mstarehe mbinguni bila huzuni tena? Waweza kujibu swali hili, ukizingatia kwamba hata wewe mwenyewe hutaki kwenda mbinguni ukakutana na uovu tena, hata uovu huo ukiwa wa ndugu au rafiki yako wa karibu!
Wengi nimesikia, wakifanyia mzaha somo la Jehanamu, wakisema kwamba watakuwa na marafiki wengi kule, na watakuwa na shughuli nyingi za kusalimiana kwa kushikana mikono na kuzungumza pamoja. Nafikiri hilo halitakuwepo. Kutokana na Maandiko kama ya Daniel 12:2 patakuwa mahali pa aibu ya hali juu, na mtu mwenye haya usoni, anayelia na kusaga meno, hataweza kumtazama mwingine, licha ya kupeana mikono. Itakuwa mahali pa vilio vya ajabu na kulaumu wale waliosaidia mtu aende pale. Hata malaika wa Shetani watamlaumu bosi wao Shetani, kwamba ni yeye ndiye aliyewafanya waingie mle. Isitoshe watu watakaokuwa katika ziwa lile la moto, kutokana na Ufunuo 21:28 ni wenye machukizo ya uongo, wanafiki, wenye viburi, waliojaa chuki, wanyonge, wauaji, wezi, wasengenyaji, wachawi, na watu wenye uovu wote. Waweza kuona uovu wako haukuwa mwingi vile, kama huo, ila

uovu ni uovu, na wote watakuwa kundi moja wakipata adhabu tofauti ila mwishowe ni kuangamizwa. Mtu hatakuwa na matamanio, au hata nafasi ya kusalimiana au kufanya lolote la furaha, kejeli, futuhi au kuchekesha kule Jehanamu.
YESU alisema katika Mathayo tano kila amwoneaye nduguye hasira imempasa hukumu, na mtu akimwapiza nduguye itampasa Jehanamu ya moto. Kama jicho au sehemu ya mwili ikikukosesha uikate na kuitupa, ni bora kuingia mbinguni na kiungo kimoja kimepungua, kuliko kwenda na mwili mzima na kutupwa Jehanamu. Kila mti usiozaa matunda hukatwa na kutupwa motoni. Aliwawambia waandishi wa mafarisayo wanamfanya mtu mmoja kuwa mwongofu na kisha kuwa mwana wa Jehanamu mara mbili kuliko wao wenyewe.

Ni jambo la uhakika, kwamba wale wanaomtumaini MUNGU, wakimtii na kuungama toba ya kweli wanapofanya dhambi, (maana hakuna binadamu asiyefanya dhambi); watakuwa na thawabu ya kuishi mbinguni kusikokuwa na kifo tena. Ila wale waovu, wasiomtumaini MUNGU au kumtii, au kuungama dhambi zao na kuzijutia watakuwa katika ziwa la moto na kiberiti alimo yule mnyama, wa Ufunuo 13, yule nabii wa uongo na Joka yule aliyewadanganya mataifa yote miaka yote yaani Ibilisi. Huko kutakuwa na mateso ya kuungua usiku na mchana (Ufunuo 20).
Jehanamu au adhabu ya waovu zimeandikwa kwa mistari michache sana kwenye Maandiko matakatifu. MUNGU amekazia upendo na mahusiano na watu Wake. Japo hatufahamu mengi kuhusu Jehanamu, kwa kusoma machache yaliyoandikwa kwenye Biblia, tunajua kwamba si mahali pazuri pa kwenda mtu. Wale wa lugha ya kingereza wakiwa hawampendi mtu wanamwambia “nenda jehanamu” au “go to hell’ Hiyo tu inatosha kutuonyesha kwamba si mahali pema. Ni pabaya mno, kuliko mahali popote pabaya tulipowahi kusikia au kwenda, ila YESU alikufa kwa kutundikwa mtini, akapata maumivu yote, ili wewe na mimi tuepuke maumivu haya makali ya Jehanamu, na tusipotee milele. Njia ya kwenda Jehanamu ni pana, ila ya kwenda mbinguni ni nyembamba. Ile ya kwenda Jehanamu mtu hana haja ya kukana nafsi au kujinyima. Waweza kufanya lolote likupendezalo kama unataka kwenda Jehanamu. Hakuna mahali Maandiko Matakatifu yanasema kwamba mkristo au muumini anayemcha Mwenyezi MUNGU anaweza kufanya chochote anachotaka kufanya. Muumini anayempenda kwa binafsi Mungu hajaruhusiwa na BWANA wake kufanya lolote alitakalo, bali lile Mwenyezi MUNGU (BWANA wetu) alilomwelekeza au Mwenyezi MUNGU alitakalo. Mkristo ni mtu anayefuata Maandiko na kuyatii. Kuhusu njia pana, huko waweza kufanya chochote utakacho ikiwemo na kuvunja Amri kumi za MUNGU.

Kwenye njia pana waweza kusema uongo, kuiba, kutoheshimu wazazi, au kutaja Jina la Mwenyezi MUNGU bure. Waweza kuwa na miungu mingine na kuiabudu. Waweza, kuacha kuheshimu Sabato ya BWANA, waweza kuacha kusali, au kwenda ibadani au kusoma Maandiko Matakatifu. Waweza kuwa na tamaa ya mali unavyotaka. Waweza kutosaidia maskini na wenye njaa, na kuwa mgomvi na asiyetii. Njia pana inachukua takataka (garbage/trash) au tabia yoyote, kama wasemavyo waswahili, “kila kitu twende tu” ila adhabu Yake ni mbaya kupita zote zinazojulikana. Hakuna mtu anayependa kuungua, kamwe. Wengi tukipata kuungua kidogo, tunakimbilia mafuta ya vaseline, asali, aloe vera, losheni au maji ya unga wa

ngano tupooze maumivu kidogo. Moto huu wa Jehanamu, hauelezeki maana kuna mawe yanayowaka na maumivu ya ajabu. Wengi walioumwa meno pia wamejua uzito wa maumivu ya meno, kutokana na maelezo haya, kusaga meno kutakuwa kubaya zaidi ya meno yanayouma au yaliyotoboka!

MUNGU ametuwekea Neno Lake pia ili tusiende Jehanamu. Maneno Yake tuliyosikia toka tukiwa wadogo, yanakuja mawazoni petu kutuvuta Kwake. Mafungu ya kukariri yaliyoganda vichwani yanatujia mara kwa mara na kutuchoma mioyo. Visa vya Biblia pia vinatusaidia turudi toka upotevuni. Maandiko ya MUNGU ni ramani, dira, taa na hekima ya kutufikisha mbinguni kwenye uzima wa milele. MUNGU hakuaidi uzima wa milele kwa wenye dhambi, bali kwa watakatifu tu. Waovu wao wameahidiwa "Jehanamu." Kitabu hichi cha Biblia kitakuweka mbali na dhambi, na Dhambi itakuweka mbali na Biblia. Mungu ametumia mahubiri pia ili kututoa katika njia ile pana ya kwenda Jehanamu. Leo ukisikia sauti Yake usifanye moyo wako kuwa mgumu. Wengi wamecheka wahubiri, wakisema staili yake ni ya kishamba, nguo zake za kimaskini, au kingereza chake si kizuri. Ila Maandiko yanasema wahubiri walitumwa ili wahubiri habari njema wala si kwa hekima ya maneno, msalaba wa Kristo usije ukabatilika. Kwa sababu Neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuuzi, bali kwa wanaookolewa ni nguvu za MUNGU. MUNGU alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa." Hata kama mtu hufikiria ana akili nyingi, na kwamba Maandiko ni maneno ya upuuzi, achunge sana maana njia hiyo ya 'kipuuzi' Mungu ameichagua ili tuokolewe tusiende Jehanamu.
Wahubiri wanaweza wasiwe na maneno ya ufasaha wala hekima, lakini cha muhimu ni sisi sote, tupate kumjua YESU Kristo aliyesulubishwa, ambaye Ndiye atakayetuokoa, twende mbinguni na kuepuka Jehanamu. Kuhubiriwa Neno la MUNGU ndiyo njia inayofanya tusiangamie. Hata hivyo binadamu wote ni watumishi walioitwa kufanya wanayopaswa kuyafanya. Pengine hilo ndilo hubiri utakalosikia mara ya mwisho katika maisha yako leo, hatujui maisha ya kesho, kwani kesho haijaahidiwa. Cha kushangaza ni kuwa vijana hufa kama wazee wafavyo. Kufa ni kwa wote. Hakutegemei umri. MUNGU ametumia maombezi ya watu, kuturudisha Kwake. Maombi ya wazazi, maombi ya watakatifu, maombi ya viongozi wa kiroho, maombi ya babu au bibi. Maombi yametuleta kwenye njia nyembamba ya kwenda mbinguni. MUNGU ametumia shida na matatizo mbali mbali kuturudisha Kwake, ili tusipotee. Ametufanya tuwe dhaifu ili tunyenyekee, na kumsikiliza.

MUNGU ametumia pia picha ya Msalaba wa YESU, tuifikirie ili tusiangamie. Kila mara ukiikumbuka picha hii, picha ya mawazo Yake, maisha Yake na siku Zake za mwisho hapa duniani, akienda kufa kwa ajili yako na yangu, sema "Yesu nakupa maisha yangu milele." Tumeandika, machache tu ambayo MUNGU ametuvuvia. Wewe waweza kuorodhesha mengine uliyopitia. Basi tuangalie pale tunapoanguka, tukatubu na kurudi. Kama tuko sawa na mahusiano yetu na MUNGU, basi tuendelee kukua hatua kwa hatua mpaka siku ile YESU atakapotokea mawinguni, kuja kutuchukua tukaishi Naye milele na milele. Itakuwa furaha ya ajabu na ya jinsi gani?

*Sala za hapa na pale yaani misimu fulani tu unapopenda, zitakufanya Upoteze


ushirikiano wako na MUNGU (sporadic)- Maombi ni pumzi ya roho. Ndiyo siri ya nguvu ya kiroho. Hakuna njia nyingine ya neema inayoweza kuwa mbadala na bado kukawa na afya ya roho na kisha mambo yakawa salama. Maombi huupatia moyo mguso wa haraka kwenye Chemchemi ya uzima, na kuimarisha mishipa na misuli ya uzoefu wa kidini/kiroho. Puuza zoezi la sala, au jihusishe na maombi bila rejareja unapotaka, hapa na pale kama utakavyo, na mara zingine usiombe kutokana na unavyoona inafaa kwako wewe binafsi, nawe utapoteza ushirika na utegemezi wako kwa MUNGU. Vitivo vya kiroho hupoteza nguvu, uzoefu wa kiroho huondokewa afya na ushupavu.

----------------------------

Maswali: Yesu amesema nini kuhusu Jehanamu? MUNGU ametusaidia kwa njia gani ili tuepuke Jehanamu? Je, Kwa nini watu hawapendi kuishi karibu na mtu mwovu? Je, MUNGU ameahidi waovu wataishi milele kwenye Neno Lake? Elezea kile Biblia inachosema kuhusu Jehanamu ilivyo.

**SIKU YA 358.**

# Jehanamu II



MUNGU amezungumzia kuhusu Mbingu kuliko Jehanamu. Mbingu ni nzuri mno, kiasi kwamba hata katika ndoto zetu nzuri mno, hakuna kinachofikia hiyo. Mbingu ni mojawapo ya wigo wa kutuzuia ili tusiende Jehanamu. Ametupa picha ya mbinguni kwenye Maandiko mara nyingi. Mwenyezi MUNGU ametuambia katika kitabu cha Waebrania “Tukifanya dhambi kusudi, baada ya kupokea ujuzi wa kweli wa Neno lake, basi haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi…Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya MUNGU aliye hai” (Waebrania 10: 26-31). Ikiwa tu mtu aliyedharau sheria ya Musa alikufa pasipo huruma kwa mashahidi wawili au watatu, Je yule anayemkanyaga Mwana wa MUNGU adhabu yake itakuwaje? Je anayemfanyia jeuri Roho wa MUNGU anapomwita, atapata neema tena? Tutafakari mambo haya, MUNGU anatupenda mno, kuliko tunavyojipenda. Hakuna awezaye kuja kwa MUNGU mwenyewe, pasipo kuvutwa na Mwenyezi MUNGU. MUNGU anatuvuta hata leo kwa njia nyingi ili tusiangamie na kwenda Jehanamu.

YESU au Mwanaadamu alikuja kutafuta na kutuokoa sisi tuliopotea, na kutoa maisha yake kwa ondoleo la dhambi zetu. YESU akikuita, ukiwa na miaka sita, kumi, kumi na tano au hata mia, usiseme kesho, kesho. Itika, ndiyo na usizitegemee akili na uwezo wako mwenyewe, bali mtegemee MUNGU kukuondolea tamaa za aina zote. Maana tamaa hizi zinatufanya tuwe mbali na mbingu ambayo MUNGU

ametuahidi. Kama umefanya dhambi, weka mambo sawa na MUNGU wako. Wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa MUNGU, ila amesema tuje kwake, na kusemezana naye, tuungame, na kuwa na toba ya kweli.

Tujisalimishe kwake na kuanza maisha mapya ndani ya YESU, tukiwa wazi kuelekezwa na mkono ule usiopungua. Njia zake MUNGU nyingi zatuweka sawa katika njia yake nyembamba, ili tusiende Jehanamu, bali tuwe na uzima wa milele. MUNGU hutumia Roho wake kutuhakikishia kwa habari ya dhambi, haki na hukumu. Pale tunapokosea, Roho wa MUNGU anazungumza nasi, na tunaisikia ile sauti ndogo. Anatuelekeza katika haki na kutukumbusha kuwa kwa kila tunalolifanya kuna hukumu, kwani maneno yetu na matendo yetu yataletwa mbele ya hukumu, hivyo ni vema kujua kwamba kila nilifanyalo ipo siku nitatoa hesabu yake. Dhambi zote zimewekwa katika mafungu matatu, tamaa za macho, tamaa za mwili, na kiburi cha maisha haya.

Mtu huvutwa kufanya mabaya kwa njia ya kutazama, na kupitia kutazama huko husikia kishawishi moyoni kwamba, mbona kitu hiki kingekuwa changu kisha anaamua kukichukua na kukifanya chake, na kwa kufanya hivyo tayari anakuwa ameiba na kuhesabiwa dhambi. Tamaa ya mwili kadhalika inaweza kumvuta mwanadamu kushiriki tendo la ndoa isivyo halali. Yeye anajua kabisa hajaoa na mpango wa Mungu ni kwamba mtu ashiriki tendo la ndoa na mke au mume wake halali. Tamaa ya mwili yaweza kuchafua mawazo na hali ya hewa kichwani na kumpelekea mwanadamu kufanya uasherati, uzinzi au ukahaba.
Kiburi cha uzima chaweka kuwa ni matumizi mabaya ya afya yako. Uko kijana na hujali mambo ya Mungu huku ukisema ngoja niponde maisha kwanza na nikisha kuzeeka nitamtafuta Mwenyezi Mungu, hiyo nayo yaweza kuwa ni aina ya kiburi cha uzima. Mungu anashauri tumtafute Yeye tungali vijana au wakati bado tuna afya nzuri. Mungu anatuvuta kwake kwa njia nyingi, picha ya mbingu ikiwa ni njia mojawapo. Anatueleza jinsi maisha kule yatakavyokuwa ya amani, furaha, mapumziko, na utukufu mwingi wa YESU, na malaika, na hata wazee wa Imani. Jaribu kupiga picha ya mbingu uone vile utakavyopungukiwa usipokuwa pale. Hakutakuwa na maumivu, machozi, huzuni wala kifo. Jambo hili ni bora kupita yote yahusuyo mbingu. Litakuwa jambo jema kuwa na YESU milele. Hii itaburudisha mioyo yetu na kuondoa wasiwasi milele.

Jambo lililomsikitisha YESU kupita yote alipokuwa karibu na kufa, ni kuhisi ametengwa na BABA yake. Ilionekana kwake utengano na BABAYE ni wa milele. YESU aliendelea mbele, na kutengwa na MUNGU, ili sisi tusitengwe naye. Kutengwa na uso wa MUNGU ni jambo baya kupita yote. Kuhusu Jehanamu yaani kutengwa milele na MUNGU, je hii ni jambo la namna gani? Hii ina maana kutakuwa hakuna lolote zuri, au tamu hata moja. Hakutakuwa na tabasamu la mtoto, hakutakuwa na mtu kukusalimia kwa furaha "habari ya leo", na wala hakuna siku nzuri ya amani. Hakuna kukutana na mtu mvumilivu, ni giza tu la utengo na MUNGU na mema yote. Itakuwa ni kulia na kusaga meno.

Pengine kwenye maumivu ya ziwa la moto, au ya kutengwa, hakutakuwa na kuona mtu karibu kwani kutakuwa na giza. Ufunuo 9 yasema malaika alipewa ufunguo wa

shimo la kuzimu na kule shimoni kukawa na moshi wa tanuru kubwa. Hatujui kwa uhakika kwamba haya ni maelezo ya kuzimu au Jehanamu. Bali kwa kufikiria tu kibinadamu hakika shimo hili lenye kina kisicho na mwisho litakuwa kitu kigumu sana. Wengi tunakuwa na woga mkubwa tukiwa tunaanguka shimoni. Hapa Maandiko yanasema hili shimo halina mwisho. Hofu hutushika tuangukapo. Tunakunja misuli yetu na kukunja sura zetu kwa sababu hakuna anayependa kuanguka kwenye shimo refu la maili nyingi, na akaendelea kushuka chini, bila kujua adhabu hii ya kuanguka itaendelea muda gani. Maelezo ya Jehanamu yanaweza kuwa kizuizi cha mwisho cha MUNGU kutusaidia ili wote tufanye maamuzi tusipotee.
Ufunuo yasema wengine walipoteza nguvu zao kutaka kuuvamia mji, wakati watakatifu watakaposhuka, wafanye vita, ila wakashindwa. Tusipoteze nguvu, kufikiria jinsi tutakavyojificha kwenye mapango au kuomba milima ituangukie ili tusipate ghadhabu au hasira ya MUNGU. Tuchukue muda sasa kufanya maamuzi ya busara ili tuwe katika Yerusalemu mpya, au mbingu mpya na nchi mpya. Wakati vitabu vitakapofunuliwa na hukumu ikiwa inaendelea, hebu tuombe MUNGU tuwe upande wake. Yawezekana tukaona inachukua muda kwa watu wema au watakatifu kushinda, ila mwishowe wema au MUNGU ndiye atakayeshinda.

MUNGU hataki kututisha na Jehanamu, ila ukianza kuifikiria mwenyewe, itakufanya uamue kwamba si mahali unapotaka kuwepo. Hebu leo basi chepuka na kuingia katika njia nyembamba kama upo njia pana. Njia pana haiko sambamba na njia nyembamba, hizi zinaenda kinyume cha nyingine. Kama hauna mahusiano na MUNGU siku ya leo, chagua ni nani unataka kumtumikia. Kuna mabwana wawili tu, Shetani au MUNGU. Ukiona unaenda njia ya chini au Jehanamu, badilisha njia pana na urudi kwenye njia nyembamba. Hebu panga kwenda mbinguni kusikokuwa na manung'uniko, magomvi, ukatili, au maneno ya kukatisha tama. Pahali pale penye amani ya milele.

MUNGU hamlazimishi mtu kuchagua kwenda mbinguni au Jehanamu, uchaguzi upo kwako na kwangu. Ila pale utakapomchagua MUNGU na kujitoa kwake kikamilifu, atafanya yote yaliyo katika uwezo wake, kukuepusha na Jehanamu au kukupa uzima wa milele. MUNGU anatumia kweli tu, na si ulaghai, kukufanya wewe umchague Yeye. Yeye hana ahadi za uongo, bali za kweli tupu. Pilato aliuliza "Kweli ni nini?" na hata leo wengi wanauliza Swali hilo. Kweli tupu na yote ni Neno la MUNGU tu. Yeye ni Njia, Kweli na uzima. Chagua njia yake, ndiyo iendayo uzimani, kwenye uzima wa milele. Leo ukisikia sauti yake usifanye moyo wako kuwa mgumu.
-----------------------------

Maswali: Tukifanya dhambi kwa makusudi baada ya kupokea ujuzi wa kweli na uzima wa milele, nini kitafanyika? Kwa nini unafikiri MUNGU amezungumzia mbingu zaidi ya Jehanamu? Leo ukisikia sauti ya MUNGU akikuita utafanyeje? Jambo baya kupita yote kuhusu Jehanamu ni nini? Roho Mtakatifu anatusaidiaje tusiende Jehanamu?

**SIKU YA 357.**
**(Desemba 22)**

# Tazama maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu.

**Ufunuo 21.**



Biblia inatueleza Yohana akaonyeshwa "mbingu mpya na nchi mpya, maana mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza imekwisha kupita, wala hakukuwa na bahari ya kutenganisha watu tena." Majangwa hayatakuwepo, makorongo, mafuriko, miiba, majani yenye sumu, nyoka au wanyama wanaodhuru wengine havitakuwepo. Hakuna kitachokufa pale, na ndiyo maana hakuna kiumbe kitakachokula kingine. Kutakuwa hakuna kuwindana. Ladha ya vitu kule itakuwa ya ajabu, kwani kila kitu kitashinda ladha za duniani humu. Macho hayajaona, wala masikio kusikia, wala kuingia katika mawazo ya Mwanadamu kuhusu uzuri wa mbingu!

Basi Yohana akaona Mji wa Yerusalemu mpya ukishuka kutoka mbinguni kwa MUNGU umewekwa tayari kama bibi-harusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Basi maskani ya Mungu itakuwa pamoja na wanadamu. MUNGU akahamisha mji Wake mkuu kule mbinguni ili akae na mwanadamu milele zote hapa duniani. Yaani mji mkuu au makao ya MUNGU yatakuwa hapa, baada ya dunia kuumbwa upya. Nasi tutakuwa watu Wake, Naye atakuwa MUNGU wetu. "Naye atafuta kila chozi" kwenye macho yetu; maana kuna huzuni nyingi duniani. Na pia wengine watakumbuka wapendwa wao walioangamia milele, iwe ni watoto wao, mama zao, baba zao, wajomba zao, shangazi zao, wajukuu zao, kaka au dada zao. Watalia, ila MUNGU atawafuta machozi.

Kutakuwa hakuna tena kifo, wala maumivu wala chochote cha kuondoa furaha. Machozi yataonekana yakiwa ya aina mbili. Machozi ya furaha na ya huzuni. Yale ya huzuni, yatakuwa mwanzoni tu. Maana twaambiwa hakutakuwa na machozi tena, wala mauti, huzuni wala maumivu, kwani MUNGU atayafuta hayo yote. Dhambi haitainua kichwa chake milele zote (Nahumu 1:9). Nabii Yohana akaambiwa andike haya na Masihi, kwani ni ya amini na ya Kweli. "Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho, nitampa yeye mwenye kiu, maji ya uzima bure." Yeye ashindaye atarithi yote hayo mema na kuishi na MUNGU milele.

Kule mbinguni kutakuwa hakuna waoga, wasioamini, wachawi, wachukizao, wauaji, wazinzi, waabuduo sanamu, wenye tabia mbovu za mbwa, waongo, au wenye uovu wowote. Hao sehemu yao itakuwa ni ziwa la moto, yaani mauti ya pili. Wale wanaompenda Mwenyezi MUNGU watakufa mauti ya kwanza hii tunayoijua ya kawaida, ila si ya pili, kwani Masihi alikufa ili tusife hicho kifo cha milele. Yohana akaonyeshwa mji mtakatifu kwenye njozi. Aliuona mji ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi MUNGU, ukiwa na Utukufu wa MUNGU na ulikuwa na mwangaza Wake mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi safi kama bilauri. Ulikuwa na ukuta mkubwa na mrefu, na milango kumi na miwili, yaani kila upande milango mitatu.



Majina ya makabila kumi na mawili yalikuwa yameandikwa kwenye milango. Na majina ya mitume 12 yaliandikwa kwenye msingi. Mji ulikuwa mraba, mapana na marefu yalikuwa sawa, na kwenda juu. Ukuta wake ulikuwa vito vya Yaspi na njia zake za dhahabu safi kama kioo kiangavu. Misingi kumi na miwili ilikuwa mawe ya vito 12 tofauti, nayo ni yaspi, yakuti samawi, kalkedoni, zumaridi, sardoniki, akiki, kristolito, zabarajadi, yakuti manjano, krisopraso, hiakintho, na amethisto. Na milango yake ilikuwa ni ya lulu.

Hakukuwa na hekalu tena maana BWANA MUNGU Mwenyezi na Mwana Kondoo ndiyo hekalu lake. Mji ule hauhitaji jua wala mwezi maana utukufu wa MUNGU huutia Nuru, na taa Yake ni Mwana Kondoo. Na watu watatembea katika nuru Yake, milango haitafungwa maana hamna usiku wala wevi au uovu. Ndani yake hakitaingia kinyonge wala afanyaye machukizo au uongo, bali wale tu walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwanakondoo. Pambano kuu litakuwa limeisha. Dhambi na wenye dhambi zitakuwa hazipo au zimetokomea milele zote. Mahusiano mazuri na furaha yatakuwa maisha ya kila siku kwa viumbe wote. Ulimwengu na sayari zote zitakuwa safi na kamilifu. Wakubwa na wadogo watasema "MUNGU NI UPENDO"

*“Bwana ni Mwenye huruma, na ni mwingi wa rehema.”Yakobo 5:11. Anasubiri kwa upendo usiochoka kusikia maungamo ya wale waliyoiacha njia na kukubali toba yao. Anatazama kurudisha kwetu shukrani, kama wakati ule mama anavyolitazamia tabasamu la utambuzi kutoka kwa mtoto wake mpendwa. Angetutaka tuelewe jinsi moyo Wake mwororo na ulio na matamanio kwetu unavyotupenda kwa dhati. Anatualika tupeleke majaribu na mitihani yetu kwenye huruma Yake, huzuni zetu kwenye upendo Wake, majeraha yetu kwenye uponyaji Wake, udhaifu wetu kwenye nguvu Zake, utupu wetu kwenye utimilifu Wake. Kamwe hakuna hata mtu mmoja aliyekatishwa tamaa aliyemjia Yeye. “Walimtazama, wakaangazwa; na nyuso zao hazikuaibika.” Zaburi 34: 5
------------------------------

Maswali: Mji mtakatifu ulikuwaje? Kwa nini hakukuwa na hekalu tena? Msingi wa mji una majina gani 12? Milango 12 ina majina gani 12? mambo gani yatakuwapo kule mbinguni? Je unapanga kwenda mbinguni?

**SIKU YA 358**
**(Desemba 23)**

# Mbinguni milele na milele.

**Ufunuo 22.**



Yohana akaonyeshwa mto wa maji ya uzima yenye kung'aa kama bilauri ukitoka katika kiti cha enzi cha Mwenyezi MUNGU na cha Mwanakondoo. Hapo upande wake kulikuwa na mti wa uzima uzaao matunda ya aina 12, utoao matunda yake kila mwezi na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa wasife tena. Laana zote zitatoweka, na kiti cha enzi cha MUNGU na Mwana-Kondoo kitakuwa ndani yake. Kutakuwa hakuna usiku tena, wala hitaji la kuwa na taa, jua au mwezi kwa kuwa MUNGU Ndiyo nuru. Wengi wetu twasema jambo la kwanza tukifika, tungetamani tumwone YESU! Bali nafikiri kwamba tungetamani sana pia kumwona MUNGU BABA na Roho Mtakatifu, maana wote hawa watupenda mno, na wameshugulikia wokovu wetu kwa hali na mali.

Basi tutamtumikia MUNGU huko kwa furaha na tutamwona uso kwa uso, na Jina Lake litakuwa kwenye vipaji vya nyuso zetu. Maneno haya ni ya amini na ya kweli, na hayana budi kuwako upesi kwani amesema "Tazama Naja upesi, heri yeye ayashikaye Maneno ya unabii ya kitabu hiki" cha Biblia. Yohana aliposikia hayo alianguka na kusujudu mbele ya miguu ya malaika aliyemwonyesha mambo haya. Naye malaika akamwambia anyanyuke maana "mimi ni mjoli" wako au mwenzako, msujudie MUNGU tu Mwana-Kondoo na si malaika. Malaika ni wajumbe na watumishi wa MUNGU kama alivyoonyeshwa Yakobo, ni ngazi inayounganisha mbingu na dunia. Hawa ni wahudumu waliowekwa kwetu na MUNGU. Kushika Maneno ya kitabu hiki inahusu pia kutojiongezea maneno yetu wenyewe au kuyapunguza. Mfano wafanya biashara ya utumwa miaka ile ya 1800, waliamua kupunguza sura za Biblia kutoka 1189 mpaka 232, nazo ndizo waliwapa watumwa

wao. Mfano kitabu chote cha Kutoka hakikuwepo kwani kilihusiana na Mungu kuwatoa Wanaisraeli utumwani. Hii ilikuwa kama robo tu ya Biblia.

Yohana akaambiwa wakati umekaribia, na ikiwa karibu kabisa, Roho wa MUNGU ataondolewa na mlango wa rehema kufungwa hii itafanya "anayedhulumu au mwenye uchafu kuzidi kuwa mwovu zaidi, ila mwenye haki na mtakatifu kuzidi kutakaswa zaidi." BWANA atakuja na ujira wake, ili kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo "heri wazifuao nguo zao" au wale wenye tabia ya mbinguni isiyo na uchafu. YESU Shina la Daudi na Nyota ile yenye kung'ara asubuhi ndiyo ametoa maagizo haya kutushuhudia leo, ili tujitayarishe. Roho wa MUNGU na bibi arusi wanatukaribisha mara tatu mbinguni wakisema NJOO! Naye asikiaye na aseme, NJOO! Naye mwenye kiu aseme njoo! (AJE), na yeye atakaye na ayatwae maji ya uzima bure".

Je wamjua rafiki, au ndugu aliyelala usingizi wa mauti? Ni huzuni kiasi gani, tunapozika wapendwa wetu. BWANA Atakapokuja, parapanda itakapolia atawaamsha watoto, wakina baba, mama, babu na bibi wote. Hii ni ahadi ya Kweli. Tutaona malaika wakibeba watoto wadogo na kuwapeleka kwa wazazi wao, na marafiki wakikutana tena uso kwa uso, na kutotengana kamwe tena. Tutawatazama waliokuwa mbinguni na kuona wale wazee wamefanywa miili yao kuwa vijana tena. Wale wagonjwa tutaona wana afya na nguvu, vipofu na viziwi na vilema wataona, kusikia na kukimbia. Kufumba na kufumbua wote tutakuwa na miili isiyokufa, na mikamilifu. Mawazo yetu yatakuwa bora kupita wakati wowote ule.

Tutajiona tukiinuliwa juu, na juu kuiacha dunia, kwenda mbinguni. Hatutakuwa na haja ya kuchukua kitu kwenda nacho kule. Hatutaona mtu akipaa kwenda mbinguni na masanduku, boti, magari, au nyumba. Kule kuna vitu vizuri zaidi na vyote tunavyovihitaji. Itakuwa safari nzuri ya utalii pia, yenye mishangao mingi. Biblia inasema tutasafiri kwa muda wa nusu saa. Kama muda huu umefuata ule unabii wa siku moja ni mwaka mmoja, basi nusu saa itakuwa siku saba hivi, na hivyo kusafiri kwenda mbinguni kutachukua siku saba. Je, mpendwa wadhani Sauli yule aliyebadilika na kuwa Paulo, atapokutana na Stefano, au Mfalme Daudi atakapomwona Uria mbinguni itakuwaje? Naamini watakuwa na muda mzuri wa kuelezana yale yaliyotokea.

Kuna wale walioishi kabla ya kusikia kuhusu habari za Mwenyezi MUNGU au za Yesu ila walimtii Roho alipozungumza nao mioyoni mwao, wakijali sheria njema za nchi zao ambazo nyingi zinaendana na Amri kumi za MUNGU. Hawa watakuwa na shauku ya kujua kuhusu habari za MUNGU na Mwana-Kondoo. Amri kumi ni nakala ya tabia ya Mungu. Watashangaa ni nini kimetokea mpaka wakaweza kuishi milele, maana hawakuwahi kusikia kuhusu ufufuo! Wale wote tuliomjua Mwenyezi na Mwana-Kondoo, wale ambao tumekuwa na Maandiko ya Neno la MUNGU tutapata nafasi ya kuwasimulia habari za YESU. Je, kuna kitu cha muhimu kweli kuliko kuwa na Mwenyezi MUNGU Milele na milele? Utajiri wa duniani ni wa muda mfupi, pengine pungufu ya mia, uzuri, kisomo, mali, umashuhuri, vyote huyoyoma, hebu tumtafute Mwenyezi Mungu Maadamu anapatikana leo!
Baada ya siku zile saba tutafika mji wa Yerusalemu. Mji mzuri kuliko tunavyofikiri,

au kuota. Ni wa mraba wa maili 1,500 kila upande. Sijui kama utakuwa na ghorofa katika urefu wake wa maili 1500 au paa lake litakuwa refu! Pengine tutakuwa na nyumba mjini, na kijijini pia ili tulime! YESU Mwenyewe atamwekea taji kila mtu kichwani mwake, na kumpa kinubi, na hata bila kujifunza au kutaabika sana, kila mmoja ataweza kucheza chombo kile nyimbo tamu za mbinguni. Wengi tusiojua kucheza vyombo vya muziki twaingojea siku hiyo! Nafikiri litakuwa jambo la kushangaza kwangu au kwetu, tukitazama, na kuona "Adamu na Mwana-Adamu wanakutana." MWANA ADAMU yaani YESU, atakaponyosha mikono Yake ya upendo kwa Adamu, na Adamu atakapoona zile alama za misumari, hakika tunafikiri kuwa ataanguka chini na kusema "Amestahili, amestahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa."

Mwana Adamu atamwonyesha Adamu bustani ile ya Edeni ambayo ilichukuliwa kwenda mbinguni kabla ya gharika, na YESU atampa matunda kutoka katika mti wa uzima. Adamu ataona mamilioni ya uzao wake walioshinda, na hili litamfanya achanganyikiwe, na kufurahi sana baada ya kuelewa vizuri sasa kuhusu kila kitu alichofanya YESU kutuokoa baada ya yeyé kuangukia dhambini. Atavamiwa na sunami (wimbi) la shukrani. Tutakapoimba wimbo wa Musa na Mwana-Kondoo na yale tuliyopitia duniani, malaika watakuwa hawawezi kuimba ule wimbo, maana hawakupitia yale tuliyopitia, na wala hawakupata uzoefu jinsi tulivyopata wokovu wetu. YESU atafungua lango la mji, na kutukaribisha. Pale tutaona meza ndefu, isiyoonekana mwisho wake, maana kila mtu aliyeshinda atakuwa pale. Pasaka iliyoandaliwa kwa ajili yetu; ya chakula kitamu ambacho YESU aliwaambia mitume "sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu." Je haungependa kuwa pale na YESU? Amua leo kuwa pale, kama ulikuwa hujaamua bado.

Tutaishi pale Yerusalemu mpya kwa miaka 1000. Huu ni wakati muhimu kwani YESU anajua tutakuwa tunawatafuta marafiki na jamaa zetu tuliotegemea tuwaone pale. Kwa masikitiko hawatakuwapo, "tutauliza wako wapi? Mbona walikuwa watu wema?" Tutafanya subira, tukiamini hukumu za MUNGU ni za haki, hapo ndipo atafungua vitabu vya kumbukumbu au rekodi na tutaangalia na kuona majina ya watu hao waliopotea. Kila dhambi yao itakuwa imerekodiwa, hata dhambi zao za siri zitakuwa wazi kwa kila mtu kuona, na tutajua kwamba kila jitihada ilifanywa kuwaokoa ila walikataa katu. Mwenyezi MUNGU hakuweza kuwasaidia kushinda dhambi zao. Walikuwa wamezificha, au wamefanya kiburi kuziungama. Hawa hawatakuwa na raha kuwa mbinguni, maana MUNGU ni moto ulao, kwa waovu, hata akiwakumbatia na kuwagusa watakuwa wanaungua. Kwa kuwa ni moto ulao palipo na dhambi. Hawatapendezwa na kutenda mema, maana wangependa kujifanyia watakavyo ili kukidhi ubinafsi wao.

Hapo ndipo tutaona kwamba MUNGU ni wa haki, na upendo, na maswali yetu yote yatakuwa yamejibiwa. Twaambiwa watakatifu tutahukumu ulimwengu kwa kuamua ipi ni adhabu halali. Watakatifu watahukumu hata wale malaika waovu (1 Kor 6:2,3), (Ufunuo 20:4). Wengi hujiuliza nini kitamtokea Shetani? Ufunuo 20 imetupa nuru kwamba Shetani au joka kuu alipatwa na mambo gani. Malaika toka mbinguni mwenye ufunguo wa kuzimu alimwendea Shetani na minyonyoro

mikubwa akamshika yule Ibilisi na Shetani na kumfunga miaka elfu na kumtupa kuzimu, asipate kumdanganya mtu tena, hata miaka elfu ikatimia. Miaka ile elfu ndiyo watakatifu walikuwa wakitalii mbinguni. Tunafikiri kwamba hii minyororo si chuma ila ni njia ya kusema kwamba hatakuwa na nafasi ya kutembea huku na kule, kudanganya watu bali atakuwa ukiwa akiwa peke yake.

Watakatifu watafurahi, wakijua Ibilisi ameliyewasumbua zaidi ya miaka 6000 ameshugulikiwa. Ukifanya hesabu ya ukoo wa YESU kwenye kitabu cha Luka utapata namba inayokaribiana na hiyo. Pengine ikifika hiyo miaka elfu sita, ule wa elfu saba utakuwa wa kuishi mbinguni unaoelezewa kama milenia kwenye Ufunuo 20, na kama ni hivyo basi kuja kwa Yesu kumekaribia sana japo hatujui miaka elfu sita inaishia lini, ila kutokana mahesabu ya mbari tutapata namba takribani na hata hivyo tunajua dalili za kuja Kwake Yesu za Mathayo 24 zote zimetimia hakika, isipokuwa ile ya habari njema kuhubiriwa. Wataalamu wa misheni wanasema watu kama bilioni tatu kati ya bilioni nane wanaoishi duniani, hawajasikia kisa cha msalaba, hebu nawe husika kwa kusema "Nitakwenda ulimwenguni kote kuwaambia watu habari njema."

Ukisikia leo dunia yetu ina miaka mabilioni usiamini, maana miaka hiyo haiafikiani na Maandiko, wala mambo mengine mengi. Mfano, Kama dunia yetu ingekuwa na miaka hiyo kusingekuwa na nafasi, maana tungekuwa na matrilioni ya watu! Hata hivyo historia tunayosoma kwenye vitabu inaanzia Mesopotamia, miaka 5000+ iliyopita takribani, hayo mamilioni yako wapi basi, na kilifanyika nini huko! Shetani atapata huzuni kifungoni, kwani hakuna wa kumjaribu, kwa sababu watakatifu watakuwa mbinguni. Hapo yeye na malaika zake watakuwa wanagombana na kulaumiana kwa nini walifanya ujinga wa namna ile. Ibilisi anajua ni yeye wa kulaumiwa kwa kila baya lililotokea kwenye sayari yetu. Akitembea duniani mwenyewe kwa ukiwa atakuwa akitafakari matokea ya uasi wake, na adhabu yake. Atakumbuka upendo wa MUNGU ulivyomvumilia na kumvuta atoke kwenye maafa, naye asisikie. Hakika naye atakiri MUNGU ni mwenye haki na upendo mwingi, na amepewa nafasi ya kutosha ila kiburi kilimjaa.

Je, umeshawahi kujiuliza kama MUNGU anatumia haki? Je umewahi kujiuliza kwa nini mambo mengine yalitokea jinsi yalivyotokea? Basi uwe na subira, ukimtumainia MUNGU wakati wa hii miaka elfu moja. Maswali yako yote hapo yatajibiwa. Swali kubwa ujiulize leo, kama alivyouliza Pilato "Nifanye nini na YESU aitwaye Kristo." Jibu la kukuokoa ni 'Tumtazame YESU, Tumtumaini na Tumtegemee Yeye. Tutembee Naye, Tukiendelea kumkodolea macho, tutakuwa kama YEYE, tutabadilishwa, kisha tutafanana Naye. Ndivyo wazungu husema 'by beholding, we become changed' Yaani kwa kumtazama Yeye tunabadilishwa taratibu ila kwa uhakika kufanana Naye!

*Roho inayomgeukia MUNGU kwa ajili ya kupata nguvu, sapoti, msaada, na uwezo, kwa maombi ya dhati ya kila siku, itakuwa na matamanio bora, uelewa dhahiri wa ile Kweli na wajibu, magoli ya kina katika utendaji kazi, na njaa na kiu ya haki ya daima. Kwa kudumisha muunganiko na MUNGU, tutawezeshwa kusambaza kwa wengine, kupitia ushirika wetu na wao, nuru, amani, utulivu, unaotawala mioyoni

mwetu. Nguvu inayopatikana katika maombi kwa MUNGU, imeunganishwa na bidii ya kudumu katika kufundisha akili kwa makini kwa kujali na kusaidia, nayo huandaa mtu kwa ajili ya majukumu ya kila siku na huweka roho katika amani katika mazingira yote


---------------------------

Maswali: Mji wa Yerusalemu mpya ni mraba wa maili ngapi? Nani wataimba Wimbo wa Musa na Mwana-Kondoo? Nini kitamtokea Shetani? Je, unajitayarisha kwenda mbinguni? Je, Umefanya nini na YESU aitwaye Kristo? Kufumba na kufumbua nini kitatokea? Roho na bibi arusi asemaje? Parapanda itakapolia itawaamsha nani? Mti wa uzima unazaa matunda mangapi? Kwa nini wa heri wafuao nguo zao kwenye damu ya Yesu? Dalili ipi za kuja kwa Bwana haijatimia?

**SIKU YA 359**
**(Desemba 24)**

# Yerusalemu mpya yashuka chini, kila goti litapigwa kwa Mwenyezi MUNGU na Kila ulimi utakiri.

**Ufunuo 20-22.**



Tumeona kwamba kwenye ile miaka 1,000 maswali yote tuliyonayo yatajibiwa. Tutaona MUNGU ni wa haki, na hukumu Zake ni za kweli, ila Shetani na malaika zake watakuwa bado wakifikiri MUNGU si wa haki. Baada ya miaka 1,000 watakatifu, watashuka wakiwa ndani ya mji mtakatifu Yerusalemu wakirudi duniani wakiwa na malaika na YESU Mwenyewe. Shetani na waovu watafufuliwa. Ufufuo huu wa pili utakuwa na miili isiyo mikamilifu na mawazo maovu kama vile walivyolala usingizi wa mauti. Hivyo waheri wafu wafao katika BWANA watakaofufuka katika ufufuo wa kwanza, ufufuo wa pili ni wa waovu.

Waovu wakimwona YESU watasema 'Amebarikiwa Yeye ajaye kwa Jina la BWANA'. Japo wanamchukia watamkiri MUNGU maana hawatakuwa na uchaguzi bali kusema kweli tu. YESU atakapokanyaga mlima wa Mzeituni, mlima utagawanyika sehemu mbili (Zakaria 14:4). Kisha Mji wa Yerusalemu mpya utashuka, huku Shetani akiuangalia na mabilioni ya waovu, walio hai tena, akifikiri kwamba ana tumaini tena la kuwa mtawala wao, naye atawaambia waovu wauteke Yerusalemu mpya. Wanapopanga kufanya mashambulizi haya amri za MUNGU zitaonekana angani nao watahukumiwa. Wataonyeshwa yote yaliyotokea, toka jaribu la Adamu, mpango wa wokovu, na kazi ya Roho Mtakatifu kuvuvia watu.

Kila mwovu atakumbuka dhambi zake, na jinsi alivyomtweza Roho wa MUNGU, na kuamini uovu wa Shetani. Kila mwovu ataona jinsi MUNGU alivyo na upendo mwingi na haki, na kwamba yeye kama mwovu anastahili kufa. Hata Shetani atakiri kwamba MUNGU ni Mwenye haki. Ufufuo hautabadili tabia ya mtu, ila

MUNGU ametupa nafasi kubadili tabia zetu sasa kwa kuukubali upendo Wake na rehema Zake. Japo waovu watakiri upendo na kusema MUNGU ni Mwenye haki, bado watakuwa wanamchukia, na hata kupanga kuteka mji. Waovu wataona Shetani ni mwongo, na watajaribu hata kuuvamia mji: ila moto utatoka mbinguni na kuwaangamiza.

Kila mwovu atangamizwa kutokana na uovu wake. Shetani atapata maumivu ya muda mrefu zaidi, ila wote wataunguzwa kuwa majivu (Malaki 4:1-3 na Ezekieli 28:19). Mbingu itakuwa salama sasa bila Shetani. Kutakuwa hakuna misafara ya maombolezo, yatima, umasikini, ajali, umbeya, dhihaka, magereza, mioto, mafuriko, volkano, ubabe, ukatili, umasikini, magonjwa, matetemeko, njaa, wizi, talaka, na huzuni au uovu wowote. Wengine hawaoni haja ya kwenda mbinguni wakisema kwamba hawataki kuishi milele kama vizuka wakielea kwenye mawingu na kupiga vinubi! Wanafikiri kama ni hivyo itachosha wengi! Ukweli ni kuwa MUNGU amepanga mema na mazuri tu kwetu. Kufurahia uumbaji, kuburudika na michoko, ni katika mengi aliyotuandalia kwani tutakuwa na miili halisi isiyoharibika na tutatambua sura za watu, uso kwa uso hakika, pale pale furaha! Ufufuo utafufua mwili, na roho Mungu Ndiye aiwekaye, pumzi ya uzima! Hakuna mwili unaotengana na pumzi ya uhai mbinguni!

Tutakuwa na muda wa kuzungumza na Adamu, Nuhu, Habili, Henoka, Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Ayubu, Musa, Eliya, Danieli, Paulo, Sulemani, Daudi, marafiki zetu, familia na wengi zaidi ya hao. Tutaweza kutembea na kuwajua viumbe katika sayari zingine, pengine zile sayari ambazo hazikuingia katika dhambi kama zetu. Mazungumzo yetu ya furaha yatahusu somo la upendo wa MUNGU, wa kumtuma Mwanawe afe na kuchukua adhabu yetu" Ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Jambo zuri ni kwamba bado tuna nafasi ya kumchagua leo hii hii, kama ulikuwa hujamchagua ili uwe na uzima wa milele, leo ndiyo siku. Ukishamchagua, wasaidie wengine pia kumchagua Mwenyezi MUNGU ili wasiangamie. Tunaokolewa ili kuokoa wengine. Una muda leo, kesho waweza kuwa umechelewa. Kesho haijulikani itakuwaje au italeta mambo gani.

Hatutakuwa na haja ya kubahatisha bahatisha yale ya milele, ni mengi MUNGU amewaandalia wale wampendao. Lakini MUNGU ametufunulia sisi kwa Roho, maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya MUNGU". Yale ametufunulia, yanatosha kutusaidia kufika mbinguni. I Wakorintho 2:9,10. Tutakuwa na nyumba kule Yerusalemu mpya, na huko kwenye nchi mpya. Tutajenga nyumba zetu, na kulima bila ya kutoka jasho. Tutarejea kwenye utaratibu wa Adamu aliyefanya kazi kabla ya dhambi, maana umande utarudi kunyweshea mimea yetu. Hakutakuwa na miiba, magugu, wadudu waharibifu au mimea ya sumu tena. Isaya 55 na 65.
Tutatembea kwenye mashamba mazuri, yenye mimea ya ajabu, na maua ya kushangaza yenye rangi zisizosemeka kwa lugha zetu za kibinadamu. Maua au mimea hayatakufa, chakula kitakuwa kitamu na wala hakitatoa uvundo, au kuoza. Hali ya Hewa itakuwa murua mara zote, mafuriko, vimbunga, mvua ya mawe, ukame au tufani hazitaonekana. Wanyama wa ajabu tutakuwa nao mule. Waweza kuamua kupanda farasi au, simba au nyangumi na wasikuangushe chini! Pengine hata wanyama watafurahi kukubeba, maana mbinguni viumbe vyote vitapendana

na kuishi kwa ajili ya kila mmoja wao. Tutasikia sauti nzuri za ndege, na pengine kutakuwa hakuna haja na kuwa na wanyama wa kufugwa kama sokwe au mbwa, kwani wanyama wote watakuwa wapole na wasio na madhara. Isaya 11:6-9.

Kwa vile hakuna kitu kitakufa tena, kamwe watu hawatakula viumbe vingine huko. Na ndiyo maana tunaambiwa hakuna kiumbe kitakuwa na maumivu tena. Hata matunda au miti, tutatumia ile sehemu tu ambayo tunahitaji, wala hatutaharibu miti au maua ambayo hatuhitaji kula au kutumia kwa ujenzi. Watu wengi sehemu zingine zenye bunduki walitengeneza bunduki wakizijaribisha kwa kuua wanyama, hata wasiwatumie kwa chakula, basi ikawa ni uharibifu, na kuumiza viumbe bila sababu maalumu. Hebu tuanze tabia nzuri ya kujali uumbaji wa mimea na wanyama kwa kuitumia kwa uangalifu. Wanyama wanajua ni nani anampenda Mungu kwa jinsi tunavyowatendea, hakuna anayempenda Mungu na kuwa mkatili kwa mnyama ambaye hadhuru!

Maji ya mito yatakuwa mazuri na masafi, kama tulivyoona mto wa uzima utatoka kwenye kiti cha enzi cha MUNGU na kwenda kwenye mti wa uzima. Mti huu utatoa matunda tofauti kila mwezi, matunda matamu yanayoponya watu wasife. Mbali na dunia yetu, tutatalii sayari na nyota zingine kama Jupita, Venusi, na Orioni na tutafurahi kuona mandhari yake. Hebu tukutane pale chini ya mti wa uzima. Ni jambo moja tu litakalotukumbusha dhambi za dunia, nalo ni makovu kwenye mikono, kichwa, na miguu ya YESU. Haya makovu yatatukumbusha kama “alitoa maisha Yake ili tusipotee bali tuwe na uzima wa milele” pale msalabani. Kwenye bustani ya Edeni MUNGU alimtembelea Adamu ‘kila jioni’, mpaka dhambi ilipoharibu mahusiano hayo mazuri, kwa miaka mingi. MUNGU ametamani kuhitimisha huu utengano. Amefanya juu chini hilo kufanikiwa.

Dhambi itakapokoma, sayari yetu itapewa heshima kuliko sayari zingine, kwa maana Mwenyezi MUNGU Mwenyewe ataishi nasi. MUNGU anataka tuwe pale. Je wewe wakubali leo ukaribisho huo wa kuwa pamoja Naye? Basi tusome Neno Lake kila siku, na kuendelea kukua kwa neema. Naye BWANA amesema tusiongeze maneno ya Biblia au kupunguza. Kwani mtu akiongeza Maneno ya MUNGU, MUNGU atamwongezea mapigo yaliyoandikwa kwenye kitabu hiki, na mtu ye yote atakayeondoa lolote katika Maneno ya unabii ya kitabu hiki, MUNGU atamwondolewa sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatatifu ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.

Wakati huu watakatifu watafurahi ajabu. Pambano kuu kati ya MUNGU na Shetani, wema na uovu litakuwa limekwisha. Dhambi na wenye dhambi havitakuwapo tena. Mpango wa wokovu utakuwa umekamilika kabisa, maana tabia ya MUNGU kila mtu atakuwa ameijua, na itakuwa wazi kabisa. Maneno Yake yataendelea milele zote. Maneno Yake ni makamilifu, na hayabadiliki. Matokeo ya dhambi yatakuwa yameeleweka. Kila mmoja atajua fika tabia ya Shetani. Kuondolewa kwa dhambi milele kutaonyesha upendo wa MUNGU na Sifa Zake za ajabu kwa uumbaji wake wote. Mahali pote sasa patakuwa salama milele.

Ujumbe wa Neno la MUNGU Biblia, ni uumbaji wa MUNGU, kuharibika kwa mambo kwa dhambi kuingia, Ukarabati wa MUNGU wa upendo kwa kumtoa Mwana Wake wa Pekee, na Kisha Kurudi kwake atuchukue tukae milele. Je uko tayari kumlaki mawinguni uishi Naye milele na milele zote? YESU anakuja upesi! Anatamani tuishi Naye milele. MUNGU Baba na Roho Mtakatifu pia wanatamani vile vile, waliishi mbinguni bila YESU kwa muda mrefu, wakijitoa mhanga kwa mengi kwa ajili yetu. Wanatungojea kwa hamu tufike nyumbani. Wameishi muda mrefu kwenye mapambano ya ukombozi wetu. Tunatamani siku moja tuimbe na MUNGU milele zote, huku tukimgusa na kuishi Naye milele zote, hii ndiyo furaha ya mbingu kupita zote na si barabara za dhahabu tu! Tunatamani turudishiwe mfano wa sura ile ya MUNGU milele zote.

Hebu tumalizie kitabu chetu kwa kutoa mwaliko wa mwisho katika Biblia tena ili kila mtu ausikie "Yeye BWANA mwenye kuyashuhudia haya maneno asema "NAJA UPESI SANA. AMINA NA UJE BWANA YESU." Roho na Bibi arusi wasema NJOO! Naye asikiaye aseme, NJOO! Naye mwenye kiu aambiwa NJOO! Na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure bure!

Neema ya Bwana Yesu na iwe pamoja nasi wote wasomaji Neno la MWENYEZI MUNGU. Watoto, vijana na wazee! Amina.

*Lakini maombi hayaeleweki kama yanavyopaswa kueleweka. Maombi yetu hayapaswi kumpa taarifa ya habari MUNGU juu ya mambo ambayo hayajui. Bwana anajua siri za kila roho. Maombi yetu hayapaswi kuwa marefu na yenye sauti kubwa. MUNGU husoma wazo lililofichwa. Tunaweza kuomba kwa siri, na Yeye anayeona sirini atasikia, na atatujazia thawabu waziwazi.
--------------------------

Maswali: Kwa nini ni hatari kupunguza au kuongeza Maandiko ya Biblia? Mtu anawezaje kupunguza au kuongeza Maandiko? Yeye Mwenye kuyashuhudia Maandiko haya anasemaje? Mambo gani unafikiri utayafurahia mbinguni? Je, ungependa kuwa katika karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo? Unajitayarishaje ili uwe kwenye karamu hiyo? Milele ina maana gani? Kwa nini mbinguni patakuwa mahali salama? MUNGU ametutayarishia mambo gani? Tunajuaje kama mbinguni ni mahali halisi?

**SIKU YA 360**
**(Desemba 25)**

# ELIMU Ya Kikristo ndiyo Elimu ya milele na bora kupita zote




Kumcha BWANA ni Mwanzo wa hekima na kumjua Mtakatifu ni ufahamu Mithali 9:10. MUNGU Ndiye chimbuko la vyote, Ndiye peke Yake Muumbaji, na Mwezeshaji wa Uhai wote kutoka chembe chembe hai moja mpaka wadudu, wanyama, nyota binadamu, malaika, falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho, Efeso 3:10. Yeye haitaji mbao au mali ghafi kutengeneza kiti au vitu, huzungumza tu na vitu huwa.

Maarifa, hekima, na ufahamu wote chimbuko lake ni BWANA. MUNGU ni upendo, na Nuru halisi, YEYE Ndiye atoaye uzima. Sheria ya MUNGU au amri Zake ni Mwalimu wetu. Soma Zaburi 119. Zaburi hii ambayo ni sura ndefu ina mashairi 22 yenye beti 8 kila moja. Amezungumza hapa mara 175 kuhusu sheria, shuhuda, amri, maagizo, Neno, njia, wosia na hukumu za MUNGU katika mafungu yake 176. Anasema ana akili zaidi ya walimu wake na wazee kwaajili ya sheria ya MUNGU, Zaburi 119:99,100. Sheria ni kioo na mwanga wa kuona gizani ili tusipotee na hivyo tutembee nuruni. Yoyote anayejali sheria na maagizo ya MUNGU atakuwa na

maisha bora na ya manufaa kuliko yule asiyejali sheria ya MUNGU.

Sote baada ya dhambi tupo kwenye pambano kuu ambalo lina pande mbili nazo ni upande wa MUNGU na upande wa shetani. Kwa vile MUNGU ni Mwenye haki, ameweka sheria kwenye hili pambano ili dunia yote ijue tabia Yake ya upendo na uchaguzi aliotupa ukilinganisha na tabia ya shetani ya uovu, chuki na udhalimu. Yabidi tutafute elimu ya MUNGU na ufalme Wake kwanza kabla ya elimu nyingine yoyote. Tukumbuke kwamba ina faida gani kupata elimu kubwa ya sayansi, injinia, uchumi au sanaa na tufe milele? Elimu ya Kikristo ndiyo ya kujipatia. Hapo Mwanzo MUNGU alianza elimu hiyo ya Kikristo katika bustani ya Edeni, aliwafundisha uso kwa uso Adamu na Hawa. Walipewa kazi, walipewa majukumu kama ya kuwapa wanyama majina, na kutunza bustani. Upendo wao, sifa na shukurani kwa MUNGU ulikuwa unakua kila siku. Mwanadamu alipewa sheria na maagizo na MUNGU.

Japo Mwanadamu alipewa maagizo na MUNGU, yeye alichagua kumsikiliza mwalimu mwovu shetani, hapo dhambi iliingia na mambo kuharibika na sasa tupo kwenye ukarabati, kujitayarisha kuingia lile darasa la mbinguni ambapo mwalimu atakuwa MUNGU tena na tutajifunza kuhusu sayari na dunia zingine na sayansi ya ukombozi milele zote.

Kutii mamlaka ya MUNGU na ya viongozi waliowekwa na MUNGU ni muhimu sana kuanzia nyumbani ambapo wazazi ndiyo walimu wa kwanza, kisha ibadani na hata katika uongozi wa serikali kama haupingani na sheria za MUNGU. Elimu ya Kweli ya nyumbani au shuleni inafundisha ibada, imani, uinjilisti na huduma. YESU anatambulishwa kama BWANA na Mwokozi na Baba YETU wa mbinguni. Wazazi walielimisha watoto wao majumbani mwao kutokana na mpango wa MUNGU kwenye maandiko, na baadaye Samweli alianzisha shule za manabii na wanafunzi walipata kufundisha Maneno ya MUNGU na kuhudumia watu katika wakati wake.

Maisha ya YESU ya utoto yatuonyesha kwamba alitii wazazi na mamlaka pia alikua akimpendeza MUNGU na wanadamu. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao kwa bidii kumcha BWANA waamkapo, waketipo,walalapo na watembeapo, KumbuKumbu la Torati 6:5. Twapasa daima kupata Elimu ya Kikristo majumbani mwetu ili tusije tukamsahau MUNGU. YESU Ndiye Mwalimu mkuu na bora kupita wote. Watu walitaka kumshika na kumshitaki ila walishindwa kwa vile walistaajabu alivyofundisha. Maisha Yake yalikuwa kielelezo na mafundisho. YESU hakika ni kielelezo chetu, hebu tuyafuate maisha Yake.

Sisi waumini, mtazamo wetu wa ulimwengu ni wa Biblia, kwamba tuliumbwa na MUNGU. Mitazamo yetu kuhusu maana ya maisha, maisha baada ya hapa, na pale tunapoelekea tunaupata kwenye Maandiko tu. Hatuupati kwenye magazeti au mila na desturi zingine kama za Uibukaji. Sisi tumeishi hapa Afrika miaka mingi na bado hatujaona sokwe kubadilika watu bado! MUNGU ataka tumwabudu katika Roho na Kweli na katika uzuri wa utakatifu Wake. Hatupaswi kuabudu dhana, nadharia, falsafa, sayansi au hisabati. Twapaswa tumche MUNGU tu na kumtukuza maana saa Yake ya hukumu imefika. Siku ya Hukumu inakuja haraka, inapaswa tuchague

elimu sahihi na inayofaa kwetu, ili siku ya hukumu tusimame bila mawaa!
Elimu na ukombozi ni kitu kimoja, kila andiko lenye pumzi ya MUNGU lafaa kwa mafundisho na kutuonya makosa yetu na kutuadabisha. Tumeambiwa tumshike sana elimu na wala tusimwache! MUNGU alituumba kwa mfano Wake ila sura hii iliharibiwa sana na dhambi, na elimu ambayo MUNGU ametupangia itarejesha sura ya MUNGU kwetu. Elimu ya Kweli lazima iondoe chuki na ubaguzi na kujua kwamba sisi sote binadamu ni watoto wa BWANA MUNGU. Tunapoinua msalaba tutaona utu na sura ya MUNGU kwa watu na kuwatendea haki, hii Ndiyo elimu ya Kweli. Elimu ya kweli inafanya tunyenyekee na tusijikuze. Sayansi ya kweli haipingi Biblia, ila nadharia potofu na za uongo ambazo ni ubunifu wa binadamu kama vile uibukaji zina hatari nyingi na ni za kupigwa vita na waumini wote.

Kazi ni mbaraka na ni sehemu ya elimu kwa mkristo. Kufanya kazi ili kupata hela na kustaafu mapema tukiwa na afya si jambo jema kwa viungo vya mwili. Mwili umeumbwa kufanya kazi. Kilimo ndiyo Alfabeti au A,Be,Che ya elimu Kazi hutupa furaha na heshima. Kufanya kazi ni zaidi ya kuajiriwa, kwani ni huduma na afya kwa mwili. Kufanya kazi za mikono kama vile mtume Paulo alivyotengeneza mahema ni sehemu ya Elimu ambayo MUNGU anataka tuwe nayo. Kilimo na kazi za mikono ni Alfabeti za Elimu ya Kikristo. Uwakili ni sehemu ya kazi ambazo MUNGU ametupa katika maisha yetu. Twapaswa kufanya kazi na kupumzika kama alivyoagiza ili tuakisi tabia Yake kila wiki.

Wazazi wengi hupeleka watoto wao katika shule za gharama kubwa kwa sababu wanataka watoto wao wawe na maendeleo mazuri ya kitaaluma, lakini shule nyingi za gharama kubwa hazina elimu ya kiroho. Matokeo yake ni kwamba wanafunzi hawa hawana elimu sawia, ambayo ni maendeleo ya nyanja za kiakili, kimwili na kiroho za mtu. Elimu hiyo inapatikana kwenye mashule yanayofundisha Maandiko. Mtu ambaye ni mzuri kimasomo, lakini mwenye kasoro kiroho hajatayarishwa kwa ajili ya ufalme ujao wa Mungu. Kwa kuongezea, mtu kama huyo hawezi kuwa raia mwema kikamilifu wa serikali za hapa duniani. Mungu awasaidie wazazi wanaomtarajia Yesu kurudi kuwapeleka watoto wao katika shule zinazofundisha Maandiko, hasa wakiwa hawajafikisha miaka 10, yaani kule ambako wanaweza kupata elimu iliyo na uwiano bora.
Soma Kumbukumbu la Torati 6 na Kitabu kinachosema Misingi ya elimu ya Kikristo, sisi tuna kopi ya mtandaoni kama hutaweza kufanikiwa kupata kopi ya kingereza, Kopi hii tumeitafsiri Kiswahili.
“Na hii ndiyo sheria, na amri, na hukumu, alizoziamuru Bwana, Mungu wenu, mfundishwe, mpate kuzitenda katika nchi ile mnayoivukia kuimiliki;

2 upate kumcha Bwana, Mungu wako, kushika amri Zake zote, na sheria Zake, ninazokuamuru, wewe na mwanao, na mwana wa mwanao, siku zote za maisha yako; tena siku zako ziongezwe.

3 Sikiza basi, Ee Israeli, ukaangalie kuzitenda; upate kufanikiwa, mpate kuongezeka sana, kama Bwana, Mungu wa baba zako, alivyokuahidi, katika nchi ijaayo maziwa na asali.

4 Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana Ndiye mmoja.

5 Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote.

6 Na Maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako;

7 nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo.

8 Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako.

9 Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako.

10 Tena itakuwa atakapokwisha Bwana, Mungu wako, kukuleta katika nchi aliyowaapia babu zako, Ibrahimu na Isaka na Yakobo, ya kuwa atakupa; miji mikubwa mizuri usiyoijenga wewe,

11 na nyumba zimejaa vitu vyema vyote usizojaza wewe, na visima vimefukuliwa usivyofukua wewe, mashamba ya mizabibu na mizeituni usiyoipanda wewe, nawe utakula na kushiba;

12 ndipo ujitunze, usije ukamsahau Bwana aliyekutoa nchi ya Misri, nyumba ya utumwa.

13 Mche Bwana, Mungu wako; Ndiye utakayemtumikia, na kuapa kwa Jina Lake.

14 Msifuate miungu mingine katika miungu ya mataifa wawazungukao;

15 kwani Bwana, Mungu wako, aliye katikati yako ni Mungu Mwenye wivu; isije ikawaka juu yako hasira ya Bwana, Mungu wako, akakuangamiza kutoka juu ya uso wa nchi.

16 Msimjaribu Bwana, Mungu wenu, kama mlivyomjaribu huko Masa.

17 Zishikeni kwa bidii sheria za Bwana, Mungu wenu, na Shuhuda Zake, na amri Zake alizokuagiza.

18 Nawe fanya yaliyo sawa, na mema, machoni pa Bwana; ili mpate kufanikiwa, nawe upate kuingia na kuimiliki nchi nzuri Bwana aliyowaapia baba zako,

19 ya kuwa atawasukumia nje adui zako wote mbele yako, kama alivyosema Bwana.

20 Na zamani zijazo atakapokuuliza mwanao, akikuambia, Ni nini Shuhuda, na amri, na hukumu, alizowaagiza Bwana, Mungu wetu?

21 Ndipo umwambie mwanao, Tulikuwa watumwa wa Farao huko Misri; Bwana, akatutoa kutoka Misri kwa mkono wa nguvu;

22 Bwana akaonya ishara na maajabu, makubwa, mazito, juu ya Misri, na juu ya Farao, na juu ya nyumba yake yote, mbele ya macho yetu;

23 akatutoa huko ili kututia huku, apate kutupa nchi aliyowaapia baba zetu.

24 Bwana akatuamuru kuzifanya amri hizi zote, tumche Bwana, Mungu wetu, tuone mema sikuzote ili atuhifadhi hai kama hivi leo.

25 Tena itakuwa haki kwetu, tukitunza kufanya maagizo haya yote mbele ya Bwana, Mungu wetu, kama alivyotuagiza."

Mara zingine mtoto anapokuwa analazimishwa kutii, anapoondoka nyumbani anafanya vile isivyo kwa kuwa ile itikadi si yake bali ni ya wazazi. Ni maombi yetu kwamba tutafanya yale ambayo yako kwenye mpango wa Mungu katika elimu yetu hapa duniani.

*Maombi ambayo hutolewa kwa MUNGU na kumweleza juu ya dhambi na unyonge wetu wote pamoja na sikitiko letu, wakati hatujisikii wanyonge hata kidogo, ni maombi ya unafiki. Ni maombi ya toba ambayo Bwana anayaangalia. "Kwa Maana Yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye Jina Lake ni Mtakatifu; Ninakaa mahali pa juu na Patakatifu, pamoja na yeye ambaye pia ni mwenye roho iliyopondeka na mnyenyekevu, ili kufufua roho ya wanyenyekevu, na kufufua moyo wa wale waliopondeka."

---

Maswali: Elimu ni nini? Elimu na Ukombozi vinahusianaje? Wana wa Israeli waliambiwa nini kwenye Kumbu Kumbu la Torati 6-fanya muhtasari? Kwanini kazi za mikono ni muhimu sana katika elimu ya Kikristo? Wokovu na elimu vinahusianaje?

**SIKU YA 361**
**(Desemba 26)**

# KUFANYA MARAFIKI WA MUNGU



Misheni au kufanya wanafunzi wa YESU ni kazi ya MUNGU, YEYE ametoa nyenzo zote za mbingu kumkomboa binadamu, ila ni kazi yetu kushirikiana Naye kwa furaha katika kazi hii ya kuokoa watu. Kazi hii si mzigo ila furaha kwa vile tunaona waliopotea wanarudi Kwake BWANA. MUNGU ameweka umilele ndani ya mioyo yetu, Mhubiri 3:1. Mtu anapozaliwa anatamani moyoni kuishi milele na MUNGU wake, anakuwa hana amani au furaha mpaka ajikabidhi kwa MUNGU. YESU ni nuru ambayo humulika kwa kila mtu, na Roho Wake Mtakatifu anatuvuta Kwake. Kila shauku ya kutenda mema huletwa kwetu na Roho Wake Mtakatifu. Japo hatumwelewi Roho Mtakatifu anavyotuvuta, Yeye ni zawadi kwetu. Binadamu alipopotea dhambini, YESU alitumwa kuja kumsaidia wakati ambapo ni mwenye dhambi. MUNGU alitutafuta hata kabla ya sisi kumtafuta. Mpango wa wokovu ulifanywa kabla ya mwanadamu kufanya dhambi. Tuna kazi ya ajabu ya kushirikiana na MUNGU kuwafanya watu wengine wawe marafiki na wafuasi wa YESU.

Kushuhudia watu wengine kunafanya watu waokolewe. Mapenzi ya MUNGU ni kila mtu afikie wokovu. MUNGU ana shauku ya wokovu wetu zaidi ya sisi. Kushuhudia ni kumwinua YESU, na kuelezea watu kile alichotufanyia kwa kutuumba na kutukomboa. Twapaswa kumwona kila mtu kama raia wa ufalme wa mbinguni, YESU anapata furaha tunapojali wokovu wa wengine. Kushuhudia ni amri ya MUNGU. Twapaswa tuwe na moyo wa urafiki na upendo na tusigombane na watu ili waone imani yetu ni kitu cha kutamanika.

Ushuhuda wetu binafsi unavutia watu, yaani yale ambayo MUNGU ametufanyia. Mioyo yetu ikiwa na upendo wa YESU tutakuwa na usongo na msukumo wa kuwaambia watu wengine habari Zake. Marko 5 yaeleza wale watu waliotolewa

pepo wakiwa tayari kumfuata YESU na kumshuhudia. Twapaswa kuwaona watu kama vile YESU alivyowaona. Kwa kuona jinsi YESU alivyofikia watu tunapata mafunzo ya kuwafikia wengine. Aliwaona watu kama raia wa ufalme wa mbinguni. Mfano Mariamu Magdalena, Mwanamke msamaria na wengine. Omba na anza ulipo, utaona mabadiliko makubwa.

Maombezi kwaajili ya watu ni muhimu sana kwa vile vita kuu kati ya Shetani na MUNGU ambayo ilianzia mbinguni inaendelea, na wengi ambao wametekwa na shetani hawana habari, hivyo wakiombewa italeta tofauti kubwa katika maamuzi yao, nao watakubali kafara ya YESU na kuwa upande wa MUNGU. YESU, Paulo, Samweli na watu wengi kwenye Maandiko wanatupa mfano wa huduma ya maombezi. Omba kwa moyo wako wote na Roho Mtakatifu atakusaidia kushuhudia. MUNGU anatoa karama mbali mbali ili kutuwezesha kushuhudia wengine. Karama za roho zinatolewa kwa kulifanya kanisa liweze kuwa na nguvu. Karama za roho ni kama vile kuhudumu, kufundisha, kutia moyo, ukarimu, huruma, msaada na roho iliyochangamka. Gundua karama ambazo MUNGU amekupa na kuzikuza.

NENO la MUNGU lina nguvu na linapotoka halitarudi Kwake tupu bali litatimiza matakwa Yake. Twapaswa kusoma Neno la MUNGU kwani linatubadilisha na linafanya tufanane Naye. Neno linafaa kwa mafundisho, na kutuondolea ujinga wote na kisha linatubariki kupita kipimo. Kuna zaidi ya ahadi 3500 kwenye Biblia. YESU alipokutana na watu walijua anawatakia mema, aliwasaidia katika shida zao, na wakawa na matumaini Naye, kisha akawaambia wamfuate, Naye akawasaidia kuwaleta watu wengine kwenye nuru ya uzima. Aliwaponya wengi, na kuwasaidia katika kile walichohitaji.

Vikundi vidogo ni msaada mkubwa katika kushuhudia, kwani hututia moyo na tunafarijiana kufanya kazi pamoja kuliko ambapo tungekuwa peke yetu. Ujumbe Mkubwa kwetu ni Kuhusu YESU! YESU ana mng'ao wa kutosha na Ndiye kiini cha imani yetu. Biblia katika ufunuo 14:6-12 inasema "Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja. Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji. Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati. Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira Yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake. Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu. Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo

yao yafuatana nao." . Ujumbe huu wa malaika hawa ni onyo kwa kile kitakachoujia ulimwengu kwa ibada na mafundisho ya uongo. Malaika hawa wanatayarisha ulimwengu wote kwaajili ya hukumu ambayo inaujia ulimwengu siku za karibuni.

*Ni lazima tupokee nuru na baraka, ili tuwe na kitu cha kutoa. Ni fursa ya kila mtendakazi kuzungumza na MUNGU kwanza katika mahali pa siri pa maombi na kisha kuzungumza na watu kama kinywa cha MUNGU. Wanaume na wanawake wanaowasiliana na MUNGU, walio na Kristo adumuye, huifanya angahewa kuwa takatifu, kwa sababu wanashirikiana na malaika watakatifu. Ushuhuda wa namna hiyo unahitajika kwa wakati huu. MUNGU Anakubali Maombi ya Kimya-Bwana atakubali hata ombi la kimya la moyo uliolemewa.

---

Maswali: Karama za roho ni kama zipi? Malaika walisema Maneno gani? Kwanini tushuhudie? Kuombea watu kunasaidia nini? Nini msaada wa vikundi vidogo?

**SIKU YA 362**
**(Desemba 27)**

# Jinsi Mungu Anavyompenda Mwanadamu



VIUMBE vyote vya ulimwengu, na jinsi Mungu alivyojidhihirisha, vyote huonyesha upendo wa Mungu. Baba yetu aliye mbinguni Ndiye Chanzo cha uhai, hekima, na furaha. Vitazame viumbe vyote jinsi vilivyo vizuri na vya ajabu. Fikiri jinsi vifaavyo kwa mahitaji na furaha, siyo ya wanadamu tu, bali ya viumbe vyote vilivyo hai. Jua na mvua, huifurahisha na kuiburudisha nchi, pamoja na vilima, bahari na mabonde, vyote hutuonyesha upendo wa Muumbaji wetu. Mungu Ndiye anayevipatia viumbe Vyake vyote mahitaji yao ya kila siku. Katika maneno mazuri ya Mtunga Zaburi twasoma haya, "Macho ya watu wote yakuelekea Wewe; Nawe huwapa chakula chao kwa wakati wake. Waufumbua mkono wako, Wakishibisha kilicho hai matakwa yake." Zaburi 145:15,16. Mungu alimwumba mwanadamu katika hali ya furaha na utakatifu kamili; na wakati nchi ilipotoka mkononi mwa Muumba, ilikuwa nzuri kabisa; haikuwa na dalili ya uharibifu wala laana ya Mungu. Taabu na mauti viliingia kwa sababu ya kuivunja sheria ya Mungu – sheria ya upendo. Lakini, hata katikati ya maumivu yatokanayo na dhambi, upendo wa Mungu umedhihirishwa. Imeandikwa ya kwamba Mungu aliilaani ardhi kwa ajili ya mwanadamu. Mwanzo 3:17. Miti yenye miiba na magugu - yaani, shida na majaribu yanayoyafanya maisha yake kuwa ya taabu na wasiwasi - yaliwekwa kwa manufaa yake, ili yawe sehemu mojawapo ya mafundisho yake yanayotakiwa katika mpango wa Mungu, ili apate kumtoa katika hali mbaya ya dhambi na kumrudisha katika hali njema aliyokuwa nayo mara ya kwanza. Ingawa dunia imeanguka katika hali mbaya kwa ajili ya dhambi, lakini yote yaliyomo si huzuni na mashaka. Viumbe vya ulimwengu vimekuwa kama mitume wa Mungu kutuletea

habari za faraja na utulivu. Kila mti wa miiba una maua yake pia; yaani, katika kila shida twaweza kupata baraka za Mungu. "Mungu ni Pendo" imeandikwa juu ya kila chipukizi, juu ya ncha ya kila jani dogo linalochipua. Ndege wazuri wanaoijaza anga na nyimbo zao za furaha, kila aina ya ua lililotiwa rangi nzuri katika ukamilifu wake likitia harufu yake nzuri katika hewa, miti mirefu sana ya msituni pamoja na majani yake mazuri ya kijani kilichokolea - yote hutushuhudia upendo na utunzaji wa Mungu, jinsi anavyotaka kuwafurahisha watoto Wake. Neno la Mungu huonyesha tabia Yake. Yeye Mwenyewe ametangaza upendo Wake na huruma Yake isiyo na kiasi/kifani. Musa alipoomba, "Nakusihi unionyeshe utukufu wako," Bwana alimjibu akanena, "Nitapitisha wema Wangu wote mbele yako." Huu ndio utukufu Wake. Bwana alipita mbele ya Musa, akatamka, "Bwana, Bwana, Mungu, mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na Kweli; Mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, Mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi." Kutoka 33:18,19; 34:6,7. Naye ni "Mwenye neema, amejaa huruma," "kwa maana Yeye hufurahia rehema."Yona 4:1; Mika 7:18. Mungu ameifungia mioyo yetu Kwake kwa namna nyingi zinazotuonyesha upendo Wake mbinguni na duniani. Kwa njia ya viumbe vya asili, na kwa vifungo vya kidunia vya upendo ambao wanadamu wanaweza kuujua. Mungu amejaribu kujidhihirisha Mwenyewe kwetu. Lakini hayo yote yanaweza tu kuudhihirisha upendo Wake kwa njia isiyo kamilifu. Ingawa ushahidi wote huo umetolewa, adui wa mema amepofusha macho ya kiroho ya wanadamu, kiasi kwamba wanamwangalia Mungu kwa hofu; wanamfikiria kuwa ni mkali na hana msamaha. Shetani aliwashawishi wanadamu wamdhanie Mungu kuwa ni hakimu mkali sana - kuwa ni mdai mkali, mwenye kuwalipiza watu bila huruma. Aliwatilia wanadamu fikara mbaya juu ya Muumbaji kwamba Yeye huangalia kwa jicho la wivu kugundua dosari na makosa ya wanadamu, ili awapatilize kwa kuwaletea hukumu juu yao. Ilikuwa ni kwa kukiondoa kivuli hicho cheusi, kwa kuuonyesha ulimwengu upendo wa Mungu usio na kikomo, ndiyo maana Yesu alikuja kuishi miongoni mwa wanadamu. Mwana wa Mungu alitoka mbinguni ili awaonyeshe wanadamu Baba aliye mbinguni. "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu Ndiye aliyemfunua." "Hakuna amjuaye Baba, ila Mwana, na yeyote ambaye Mwana apenda kumfunulia." Yoh. 1:18; Mathayo 11:27. Mmoja wa wanafunzi Wake alipomwambia "Tuonyeshe Baba," Yesu alimjibu, "Nimekuwa pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona Mimi, amemwona Baba; wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba?" Yoh. 14:8,9. Yesu alipoeleza kazi yake aliyokuja kufanya hapa duniani, alisema hivi, "Roho wa Bwana Yu juu yangu; Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa." Luka 4:18. Hiyo ndiyo kazi Yake. "Naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja Naye." Matendo 10:38. Palikuwa na vijiji vizima ambamo hamkusikika kilio cha ugonjwa katika nyumba yoyote; maana alikuwa amevipitia, na kuwaponya wagonjwa wao wote. Kazi yake ilishuhudia kutiwa mafuta Kwake na Mungu. Katika kila tendo la maisha Yake yote alionyesha upendo, wema na huruma; moyo Wake ulionyesha kwa wanadamu huruma Yake yenye kuwasikitikia. Alikuwa katika hali ya kibinadamu, ili apate kukidhi mahitaji ya wanadamu. Maskini hohe hahe na walio duni kabisa hawakuwa na hofu yo yote kumwendea. Hata watoto walivutwa Kwake. Walipenda

kupanda juu ya magoti Yake, na kuukodolea macho yao uso Wake uliojaa mawazo mazito, fadhili na upendo. Yesu hakuficha neno lolote la Kweli, lakini aliyasema yote kwa moyo wa upendo. Alitumia busara sana na uangalifu na huruma katika maongezi Yake na watu. Hakuwafanyia watu jeuri kamwe, hakusema maneno yoyote makali yasipohusu, hakuwahuzunisha watu bila maana. Hakuulaumu udhaifu wa kibinadamu. Alisema Kweli tupu, lakini alisema yote kwa moyo wa upendo. Alichukizwa sana na hali ya unafiki, na kutokuamini, na uovu; lakini kila aliposema maneno ya lawama na mashtaka, aliyasema kwa masikitiko makubwa. Aliulilia Yerusalemu, mji alioupenda, ambao ulikataa kumpokea Yeye aliye Njia, Kweli, na Uzima. Walimkana Yeye aliye Mwokozi, lakini hata hivyo akazidi kuwahurumia. Maisha Yake yalikuwa ya kujinyima Mwenyewe na kuwafikiria wengine. Kila mtu alikuwa na thamani kubwa machoni Pake. Ingawa alijionyesha daima kuwa ana hadhi ya Mungu, hakumdharau mwanadamu yeyote wa familia Yake Mungu. Aliwaona watu wote kuwa ni watu walioanguka ambao alikuja kuwaokoa. Hiyo ndiyo tabia Yake Kristo kama ilivyofunuliwa katika maisha Yake. Hiyo ndiyo tabia ya Mungu. Ni kutoka katika moyo Wake Baba vitokako vijito vya huruma ya Mungu, iliyoonekana ndani ya Kristo, vitiririkavyo kwenda kwa wana wa wanadamu. Yesu, Mwokozi aliye mwema, Mwenye huruma, Ndiye Mungu hasa "aliyedhihirishwa katika mwili" wa kibinadamu. 1 Tim. 3:16. Ilikuwa ni kwa ajili ya kutukomboa sisi Yesu aliishi na kuteswa na kufa. Alikuwa "mtu wa huzuni nyingi" (Isa. 53:3), ili tuwe washiriki pamoja Naye katika furaha ya milele. Mungu alimruhusu Mwanawe Mpendwa, aliyejaa neema na Kweli, kuja kutoka kwenye utukufu usioelezeka, na kufika hapa duniani, palipoharibika kwa ajili ya dhambi, palipotiwa giza kwa kivuli cha mauti na laana. Alimkubalia atoke mahali anapopendwa na Babaye na kusifiwa na malaika, aje kuaibishwa, kutukanwa, kudhalilishwa, kuchukiwa, na kuuawa. "Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Isa. 53:5. Mwangalieni akiwa jangwani, katika bustani ya Gethsemane, tena juu ya msalaba! Mwana Mtakatifu wa Mungu akachukua Mwenyewe uzito wa dhambi ya wanadamu. Yeye aliyekuwa na umoja na Mungu, akauona Mwenyewe moyoni Mwake ubaya wa kutisha wa ile hali ya kutengana na Mungu, ndiyo hali ya wanadamu kwa ajili ya dhambi. Kwa ajili ya matengano hayo akaona uchungu moyoni Naye akalia, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Mathayo 27:46. Uzito wa dhambi, jinsi ulivyo mbaya kupita kiasi, na jinsi ulivyoleta kutengana na Mungu - huu ndio uliouvunja moyo wa Mwana wa Mungu. Lakini Yesu hakujitoa kuwa dhabihu kubwa hivi kwa madhumuni ya kumfanya Baba Yake awe na moyo wa kuwapenda wanadamu, wala si kwa kumfanya apende kuwaokoa. Sivyo kabisa! "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yoh. 3:16. Tangu zamani Baba yetu aliye mbinguni ametupenda, si kwa ajili ya upatanisho alioufanya Yesu, ila kwa kuwa Mungu Mwenyewe alitupenda, Naye akamkubali Yesu afanye upatanisho huo. Kristo Ndiye njia ambayo kwayo Mungu hutuonyesha upendo Wake kwetu. "Yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake." 2 Kor. 5:19. Mungu alipata maumivu pamoja na Mwanawe. Katika maumivu makali ya Gethsemane, na kifo Chake pale Kalwari, moyo ule wenye Upendo wa milele ulilipa fidia ya ukombozi wetu. Yesu alisema, "Ndiposa Baba anipenda, kwa sababu nautoa uhai Wangu ili niutwae tena." Yoh. 10:17. Yaani, ni kama Yesu angesema hivi: "Baba Yangu amewapendeni

sana hata anazidi kunipenda Mimi kwa sababu ya kujitoa maisha Yangu kwa ajili ya kuwakomboa ninyi. Mimi nikijitoa kuwa badala yenu na kuwa mdhamini wenu, na kuyasalimisha maisha Yangu, na kuchukua madeni yenu, na makosa yenu, Baba Yangu huzidi kunipenda; kwa sababu kwa ajili ya dhabihu Yangu, Mungu aweza kuwa Mwenye haki, tena Mwenye kumhesabia haki yule amwaminiye Yesu." Hakuna awezaye kutuokoa, ila Mwana wa Mungu peke Yake; kwa kuwa ni Yeye pekee aliyekuwa pamoja na Baba, awezaye kuitangaza tabia Yake. Ni yule tu aliyekijua kimo na kina cha upendo wa Mungu, Ndiye angeweza kuudhihirisha upendo ule barabara. Hakuna njia nyingine ya kutuonyesha jinsi Mungu anavyowapenda wanadamu waliopotea, ila kwa njia hii moja tu, yaani ya Kristo alivyojitoa na kufa badala yao. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee."Yoh. 3:16. Mungu alimtoa Mwanawe sio kwa ajili ya kuishi tu kati ya wanadamu, kuzichukua dhambi zao, na kufa kama kafara yao. Alimkabidhi kwa jamii ya kibinadamu iliyoanguka. Kristo alitakiwa kushirikiana nao katika mambo ya maisha yao na haja zao zote. Yeye aliyekuwa umoja na Mungu amejifungamanisha na wanadamu kwa vifungo visivyoweza kuvunjwa kamwe. Yesu "haoni haya kuwaita ndugu Zake." (Ebr. 2:11); Yeye Ndiye Dhabihu yetu, Mwombezi wetu mbele za Mungu, Ndugu yetu aliye katika mfano wa kibinadamu hata mbele ya kiti cha enzi cha Baba, na kuwa na umoja nao hao ambao amewakomboa milele zote - Yeye Ndiye Mwana wa Adamu. Alifanya hayo yote ili amkomboe mwanadamu kutoka katika dhambi na hali yake mbaya, ili mwanadamu naye apate kuuonyesha upendo wa Mungu na kushirikiana Naye katika furaha ya utakatifu. Tukifahamu kima cha wokovu wetu, jinsi Mwana wa Mungu alivyokufa kwa ajili yetu, imetulazimu kutambua jinsi tunavyoweza kuwa watu walio bora katika Kristo. Mtume Yohana alipofahamu upendo wa Mungu jinsi ulivyo mkubwa mno, aliona hana budi kumcha Mungu na kumsujudu moyoni mwake. Upendo huo, jinsi ulivyo wa huruma na rehema, ni upendo mkubwa usioweza kusemeka; naye Yohana alisema, "Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo." 1 Yohana 3:1. Mungu amewaona wanadamu kuwa ni wenye thamani kubwa ya namna gani! Kwa kuanguka katika dhambi, wanadamu wakawa chini ya mamlaka ya Shetani. Lakini kwa kuiamini kafara ya upatanisho aliyoitoa Kristo, wana wa Adamu waweza kuwa wana wa Mungu. Kristo alikuwa katika hali ya kibinadamu, ili apate kuwasaidia wanadamu. Wanadamu walioanguka wamewekwa mahali ambapo, kwa njia ya kujiunganisha na Kristo, wanaweza kweli kugeuzwa hali yao, na kustahili kuitwa "wana wa Mungu." Ni upendo wa ajabu huo, hauwezi kulinganishwa na kitu cho chote! Wana wa Mfalme aliye mbinguni! Ahadi ya thamani! Ni jambo la maana lifaalo kufikiriwa sana! Upendo wa Mungu usio na kifani kwa ulimwengu usiompenda! Fikara hiyo huulainisha moyo na kuiteka nia ili ipatane na mapenzi ya Mungu. Na kadiri tunavyozidi kuichunguza tabia ya Mungu katika nuru ya msalaba, ndivyo kadiri tunavyoona zaidi rehema, upole, na msamaha vikichangamana na usawa na haki, na ndivyo kadiri tunavyotambua zaidi ushahidi mwingi sana wa upendo Wake ambao hauna mwisho, na huruma Yake ipitayo huruma ya mama iliyojaa shauku kwa mtoto wake mtukutu. (Kutoka kitabu cha Njia salama.) Hebu tuanze siku yetu na Maombi, kuomba ni kuzungumza na Mungu, kama vile tunavyozungumza na rafiki. Tumwambie haja za mioyo yetu, furaha, huzuni na changamoto zetu, Yeye Yupo tayari kusikiliza. Kuna mambo mengine hatutapata mpaka tuombe kwaajili ya pambano kuu Kati ya Mungu na

Shetani, Tumwambie Mungu haja zetu kila siku na tuwasiliane Naye bila siku nzima mioyoni mwetu.

*Tumia Lugha Rahisi katika Maombi-Lugha yenye misamiati migumu au mingi, yenye madoido mengi, yenye sauti ya juu ya kujifanya na yenye maelezo mengi haifai katika maombi, iwe ombi hilo linatolewa kwenye mimbari, kwenye mzunguko wa familia, au kwa siri. Hasa yule anayetoa ombi la hadharani anapaswa kutumia lugha rahisi, ili wengine waelewe yanayosemwa na kuungana na ombi hilo. Ni sala inayotoka moyoni kwa imani, ndiyo ambayo husikika mbinguni na kujibiwa duniani.

--------------------------------

Maswali

Elezea upendo wa Mungu katika maisha yako na wale wanaokuzunguka

**SIKU YA 363**
**(Desemba 28)**

# Pambano kuu limekwisha! Vidogo na vikubwa, hai na visivyo hai vyasema Mungu ni Upendo!



Shangwe shangwe zitakuwa mbinguni, wala macho hayajaona wala masikio kusikia wala kuingia katika mawazo ya binadamu yale MUNGU amewatayarishia binadamu, hakuna dhiki wala maombolezo! Pale Haleluya za Wayahudi na Hosana za Mataifa zitachanganyika, itakuwa siku ya ajabu! MUNGU atusaidie wapendwa wanapofufuka tuonane nao ufufuo wa kwanza! Pale kutakuwa na kuvishwa mwili wa Kutokufa, tutasema mauti ku wapi kushinda kwako?! Jamani nafikiri siku hiyo Ushindi wa Pendo la Mungu , pendo la Mungu alilopanda Mwenyewe mioyoni mwetu litakamilika. Ushirikiano na viumbe vitakatifu, na umoja wa haki usio na kasoro, jamii yote ya mbinguni na ya duniani vitadumisha furaha ya milele iliyo kamili, Waefeso. 3:15. Hapo katika mawazo makamilifu tutaona maajabu ya uwezo wa Mungu wa kuumba, na siri za upendo wa ukombozi. Kila kiungo kitakuwa na kuendelea.

Maarifa ya kujifunza hayatakua na kikomo. Upendo wetu utaendelea kukufa kila siku, mahusiano yetu yataboreshwa kila siku. Mambo makuu ya ajabu yatafikiwa na hali ya juu ya mawazo na vifiko vyote vitafikiwa. Hata hivyo kutakuwa na mambo mengi ya ajabu ya kupekua. Milele na milele zote kutakuwa na mafunzo yasiyo na mwisho wala hakutakuwa na kuchoka. Hazina zote za Mungu zitafunguliwa kwa wana wa Mungu waliokombolewa. Watatembea dunia nyingine bila kuwa na safari za kuchosha. Wana wa nchi hii wataingia katika ulimwengu wa wasiokuwa na dhambi na kushiriki maajabu ya elimu yao isiyokuwa na kasoro, ambayo wao wamekuwa nayo vizazi kwa vizazi. Wataangalia utukufu wa uumbaji bila kuwa na kiwi machoni. Na jua, nyota na sayari zote zikikizunguka kiti cha enzi. Kadiri miaka ya milele inavyokwenda, ndivyo ufunuo wa utukufu wa katika miaka ya umilele inapoendelea, itazidi kufunua utukufu wa Mungu na wa Kristo. Jinsi mwanadamu atakavyopata elimu hii ya kumjua Mungu, Ndivyo kutakavyo kuwepo kufanana zaidi Naye kitabia.

Mungu na Kristo watatufunulia kwa ajabu. Kwa kadri watu watakavyojifunza tabia ya Mungu ndivyo watazidi kumwabudu na kumpenda. Kadri Yesu anavyowafunulia siri za ukombozi wa vita kuu kati ya wema na ubaya ulivyoletwa na shetani, ndivyo watakavyozidi kumtukuza na kumtumikia kaw moyo wao wote, na kumwimbia kwa sauti za watu maelfu mara maelfu makumi, "Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari na vitu vyote vilivyo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na Yeye Mwana Kondoo hata milele na milele" ufunuo 5:13 Mapambano makuu yamekoma. Dhambi na wenye dhambi hakuna tena. Ulimwengu mzima sasa umeshafika mbinguni. Umoja na ushirikiano ulio kamili kabisa umeenea mbinguni. Kutoka kwa Muumbaji hufurika uzima, nuru na furaha na kuenea mahali pote. Tangu kwa kitu kidogo mno (atomi ndogo) mpaka kwa kikubwa kilinganacho na ulimwengu mzima, vitu vyote, vilivyo hai na visivyo hai, katika hali yote, hutangaza kuwa Mungu ni Pendo.

Mungu atujalie nasi upendo wetu, kwani siku moja mbinguni utasheheni zaidi na utaendelea kuongezeka kwani tutagundua yale aliyotufanyia na kupata mshangao wa ajabu.
(PambanoKuu)

Hebu turudie tena faraja hii ya Ufunuo 22:17 "Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure". Bure kabisa!

*Ni Fursa yetu Kupiga Magoti Wakati wa kusali- tunapokuwa katika umma na katika ibada binafsi ni fursa yetu kusujudu kwa kupiga magoti mbele za MUNGU tunapotoa maombi yetu Kwake. Yesu, mfano wetu, "alipiga magoti na kuomba." Luka 22:41. Juu ya wanafunzi Wake imeandikwa kwamba wao pia, "walipiga magoti na kuomba." Matendo 9:40. Paulo alitangaza, "Ninampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti." Waefeso 3:14. Katika kuungama mbele za MUNGU dhambi za Israeli, Ezra alipiga magoti. Tazama Ezra 9: 5. Danieli "alipiga magoti mara tatu kwa siku, akasali, akashukuru mbele za MUNGU wake." Danieli 6:10.

*Maombi Yetu Hayawezi Kupotea—Ni jambo la ajabu kwamba tunaweza kuomba kwa ufasaha na ufanisi; yaani kwamba, sisi wanadamu tusiostahili, tunaokufa na wakosefu, tunao uwezo wa kutoa maombi yetu kwa MUNGU. Je! Ni nguvu gani ya juu zaidi ambayo mwanadamu anaweza kiutamani kuliko hii basi, - kuwa na ushirika na MUNGU asiye na kikomo? Mtu dhaifu, na mwenye dhambi ana nafasi na upendeleo wa kuzungumza na Muumba wake. Tunaweza kutamka maneno ambayo yanakifikia kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu (sayari zote-Universe). Tunaweza kuongea na Yesu tunapotembea njiani, Naye anasema, Mimi Niko mkono wako wa kuume.

*Omba, kisha; omba, nawe utapokea. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, ongezeko la imani. Kwa kila ombi la dhati jibu litakuja. Linaweza lisije vile vile unavyotamani, au kwa wakati unaolitafuta; lakini litakuja kwa njia na kwa wakati ambao utakidhi mahitaji yako kwa ubora zaidi. Maombi unayotoa katika upweke, katika uchovu, katika majaribio, MUNGU hujibu, sio kila wakati kulingana na matarajio yako, lakini daima kwa faida yako.

*Wakina baba na wakina mama hata shuguli zenu ziwe nyingi kiasi gani, chukueni muda kuomba. Katika jitihada zetu za kuwafariji, kuwahudumia na kuwafurahisha wageni, hebu tusipuuze wajibu wetu kwa MUNGU. Saa ya maombi haipaswi kupuuzwa kwa kuzingatia jambo au mtu yeyote. Msizungumze na kujifurahisha wenyewe hadi mchoshwe kabisa kufurahia msimu wa ibada. Kufanya hivi ni kumtolea MUNGU sadaka iliyo kilema. Saa za mapema za jioni, wakati ambapo tunapoweza kuomba bila harakaharaka na tukiwa katika ufahamu wetu (akili inafanya kazi vyema), tunapaswa kuwasilisha dua zetu na kupaza sauti zetu kwa furaha, tukimsifu Mungu na kumpa shukrani zetu.

---

Maswali: Elezea maana ya pambano kuu, Kwanini dhambi na wenye dhambi hawatakuweko tena

**SIKU YA 364**
**(Desemba 29)**

# Jinsi ya kukuza Ubongo wako ili uwe na Akili sana (genius) Kwa kutafakari yale ya Mbinguni na kuyafanyia kazi, hatua kwa hatua



1. Fikiri: Kama ambavyo mazoezi ya viungo humsaidia yeye afanyae, ndivyo nawe inavyokuwa unapoizoesha sehemu ya mbele ya ubongo wako kufikiri, uwezo wako wa kufikiri unaongezeka.

2. Kuwa mtu anayependa ukweli, kuwa na shauku nao, MUNGU hana ukomo, Naye huudhihirisha upendo Wake kwetu kila siku (Maandiko, Sayansi na uzoefu). Atakuonyesha Kweli katika fani zote, iwe ni sayansi au mengineyo.

a. Jifunze na ufurahie Amri za Mungu na kanuni Zake. Sheria ya Upendo, Sheria ya uhuru.

3. Zithibitishe nadharia zote kuhusu Mungu kwa kutumia maandiko, usifuate ubunifu wa mwanadamu kama vile Uibukaji. Mtumaini BWANA kwa akili zako zote wala usizitegemee akili zako mwenyewe, katika njia zako zote mkiri YEYE Naye atakusaidia katika njia zako zote.

4. kwa kulingana na ushahidi wa tabia ya Mungu Uaminifu wa kiwango cha juu na tabia ya upendo, jisalimishe Kwake, umkaribishe moyoni. Anza kila siku kwa kumualika Roho wake. Jitoe wakfu Kwake ukae ndani Yake, Naye atakaa ndani Yako. Mwulize Roho Wake afanye makazi ndani Yako.

5. Tafakari kila siku kuhusiana na tabia ya Mungu ya upendo na ufahamu, Ukweli uliojazwa na shukrani, na tafakari juu ya Mungu na ufalme Wake wa upendo na kazi ya uumbaji.

6. Mwamini Mungu katika maisha yako leo, na siku za usoni na matokeo yake baada ya kuelewa uaminifu Wake na kupitia uzoefu Wake.

7. Fanya mazoezi ya kanuni za Mungu. Ishi bila choyo, kwa kuwapatia wengine, jitolee na tafuta kuwashirikisha wengine kile Mungu alichokupa. Kadri unavyotoa ndivyo utakavyopokea.

8. Tafuta namna ya kushiriki ukweli kuhusiana na ufalme wa Mungu na upendo kwa wengine, jiunge na taasisi zinazojishughulisha na kudhihirisha upendo wa Mungu ulimwenguni. Anzisha huduma, ongoza masomo ya biblia, shirikiana na waumini mlio na mtizamo sawa wa kiimani. Ushirika hukuza uwezo na maarifa, hudhihirisha upendo wa Mungu katika kuponya na kukuhuisha.

9. Ishi kwa kulingana na mpango wa Mungu wa maisha ya kimwili. Jiepushe na sumu zinazoweza kudhuru mwili na roho kama vile, tumbaku, pombe, madawa ya kulevya, viburudisho, uraibu, michezo ya kupigana, kusoma vitabu vya kidunia, ama mambo yanayohafifisha tabia ya Mungu.

10. Fanya mazoezi ya mara kwa mara ya viungo na ukuaji wa mishipa ya fahamu, pamoja na chembechembe za kusawilisha kiwango cha hasira.

11. Pata muda wa kutosha wa kupumzika, kunywa maji, vuta hewa, kula vizuri na kulala ili kwamba ubongo wako usije ukaathirika katika uwezo wake wa kufanya kazi.

12. Ishi kwa kulingana na kanuni ya Mungu ya Asili. Kula vyakula vyenye afya, hakikisha unatoa uchafu mwilini, pata mwanga wa jua, utapunguza magonjwa mengi.

13. Samehe: usishikilie jambo kifuani, Kutunza hasira kifuani kunakufanya kuwa mtu wa hofu na mashaka na hatimaye hupunguza amani na afya kwako. Ondoa chuki moyoni, na mawazo machafu au hila kwa watu.

14. Usiwe na hatia: inapunguza Amani, na kuongeza mashaka, na inawathiri wengine wasio na hatia, ungama dhambi zako na endelea na maisha ukiamini umesamehewa, nawe jisamehe.

15. Kama hofu na mashaka imekujaribu ili kutenda kinyume na dhamiri yako ili kwamba upate ukubali wa wenzio, kumbuka kujiweka pembeni na kujiuliza.

a. Ukweli ni nini? Kipi ni sahihi? Kipi kina afya? Na kipi kinastahili? Je nifanyeje?

b. Jiulize mwenyewe endapo mtu fulani amekukataa ama amekukasirikia kwa kufanya kile unachoamini kuwa ni sahihi je, huyu aweza kweli kuwa ni rafiki yako, je unahitaji ukubali wao?

c. Kuwa tayari kuwaweka watu wengine huru kufikiri ama kuhisi kadri watakavyo kuhusiana na wewe. Endapo unafikiri “kama nikifanya kile wanachohitaji, basi hawatanikasirikia”. Basi jaribu kuwaacha huru wafikiri kadiri wanavyochagua

kufikiri juu yako na utakuwa huru kutokana na misongo ya kutaka kuridhisha matakwa yao.

d. Kumbuka upendo hufanya kile kilicho sahihi kiafya na kimantiki, kwakuwa ndivyo, si kwa kuwa inasikika vizuri wakati huo. Tazama ng'ambo na utumie kanuni hizi za Mungu hata kama zinaonekana kuwa ngumu kwa wakati huo.

e. Daima MTAZAME YESU, ishi kwa ujasiri katika uzuri wa MUNGU, ukijua Ukweli wa SHERIA YAKE ya upendo, mpango wa maisha, kwa moyo wako wote itazamie siku ya YA MAREJEO YAKE na Pentekoste Yake maishani mwako kila siku.

Daima tujiulize mambo haya tunapoendelea. Kumpenda Mungu haina maana kwamba hatufanyi dhambi kabisa, maana sisi ni binadamu nasi tunakosea hakika. Na si matendo mabaya au mazuri tunayofanya hapa na pale, bali ni kule tunakoegemea zaidi, yaani mwelekeo wetu upo wapi daima. Hakuna aliyeokolewa kwaajili ya matendo yake, wokovu ni zawadi toka kwa Mungu. Matendo ni tunda la wokovu, na tutatona kwamba alituokoa na hivyo hatuna haja ya kuwa na miungu au utumwa mwingine wa sanamu. Ni nani anayeutawala moyo wangu? Fikara zangu ni juu ya nani? Nimezoea kuongea juu ya nani? Ni nani ambaye nampenda kuliko wote na kumtumikia kwa nguvu zetu zote? Kama sisi tu watu wa Mwenyezi Mungu, basi, fikara zetu zi pamoja Naye, na fikara zetu tamu sana zitakuwa juu Yake. Tunajitoa Kwake pamoja na vyote tulivyo navyo mara zote. Twatamani kufanana Naye, kuwa na Roho Wake mioyoni, kufanya mapenzi Yake na kumpendeza katika mambo yote. Wale wanaokuwa viumbe vipya katika Kristo Yesu watazaa matunda ya Roho hakika!

Akiwa uhamishoni kwenye kisiwa cha Patmo, Yohana alihisi kwamba manufaa yake kwa Bwana yalikuwa yamefikia ukomo. Ila alipata mshangao mkubwa. Katika mazingira hayo yenye utata, Yesu Kristo alimfunulia Yohana maono ambayo yalieleza kwa kina matukio ya wakati ujao. Mungu humtumia amtakaye, wakati wowote na popote apendapo.Hebu uwe na matumaini na unoe ubongo wako, ili Yesu akutumie, hata pale ambapo unaona mambo hayawezekani!

*Hebu wote wanaowatembelea Wakristo waone kwamba saa ya maombi ni ya thamani zaidi, takatifu zaidi, na saa ya furaha zaidi ya siku. Misimu hii ya ibada huwa na uboreshaji, usafishaji, ushawishi unaoinua juu ya wote wanaoshiriki. Huleta amani na pumziko la shukrani kwa roho . Asubuhi na jioni ulimwengu wa mbinguni unaitazama kila kaya inayoomba, na malaika aliye na ubani, akiwakilisha damu ya upatanisho, hutafuta njia ya kumfikia MUNGU.

---

Elezea njia 10 za kukuza ubongo wako, na kuelezea leo hivi unafanya nini kuhusu kukuza ubongo wako.

**SIKU YA 365**
**(Desemba 30)**

# Hatua za ufanisi katika maisha yako



Hatua ya 1: Amka masaa mawili kabla ya miadi yako ya kwanza au kabla ya kufika kazini. Wekeza masaa ya mwanzo kwa kusoma vitabu vya kiroho, Anza na NENO la MUNGU, kisha vingine vya Elimu na vya kutia hamasa. "Masaa ya kwanza ndio gurudumu la kuendesha siku"

Hatua ya 2: Andika tena malengo yako makuu kila siku katika daftari katika wakati uliopo kila asubuhi kabla ya kuondoka, bila kuangalia kile ulichoandika jana. Kitendo cha kuandika na kurudia ni cha kuunda kanuni ya uundwaji wa taarifa katika mfumo wa kuongoza akili yako. Unaporudia kuandika malengo kumi kila asubuhi utaendelea kuona na kufikiri juu ya fursa za kufikia malengo hayo hatimaye. Utakuwa makini, mwenye mwelekeo sahihi na usiyeyumbishwa, utakuwa mtu mwenye malengo na nia thabiti. Na utafanikiwa katika malengo yako kwa haraka zaidi kuliko kama yangekuwa ni mawazo tu yanayoelea katika akili yako.

Hatua ya 3: Kila siku weka mipango mapema. Andaa orodha na panga vipaumbele katika siku yako kabla ya kuondoka nyumbani. Uwezo wako wa kuona vipaumbele

na kuchagua kile ambacho ni cha muhimu zaidi ambacho utakuwa ukifanya kila wakati ni ufunguo wa kupangilia maisha yako na kuzidisha matokeo yake.

Hatua ya 4: Jenga nidhamu ya kushughulisha akili yako yote katika jambo MOJA. Chagua kitu ambacho ni cha muhimu kuliko vyote ambacho unaweza kufanya kila siku. Halafu anza nacho kwanza na kifanyie kazi mpaka kimekamilika kwa 100%. Uwezo wako wa kuwa makini na kufanya kazi, wakati unaendelea na na zoezi la kujijengea hiyo kuwa tabia, yenyewe, itakuwezesha kukuza uzalishaji wako, elimu ya Kiroho, ufanisi, na matokeo mazuri.

Hatua ya 5: Sikiliza vipindi vya kuelimisha katika simu, video au radio, piga marufuku vipindi vyenye matusi, dhambi, kupoteza muda na futuhi n.k: Unapogeuza nyumbani kwako kuwa darasa unapata elimu sawasawa na kuhudhuria mihula miwili ya masomo ya shuleni/chuoni wakati. Watu wengi husema ukitumia masaa matatu kujifunza kitu fulani, baada ya miaka mitatu utakuwa na elimu inayolingana na mwenye shahada ya kitu hicho. Mfano kila siku ukichukua kusomea Kilimo kwa bidii, yaani masaa matatu kwa siku, na kuangalia mitaala na kutenda hayo n.k, utakuwa na shahada ya kilimo kichwani baada ya miaka mitatu, waweza usiwe na cheti, bali utakuwa umeelimika na uwezo wako utakuwa ule wa mwenye shahada. Watu wengi wamebadilika toka hali ngumu na kupata stadi za maisha kama ujasiliamali, ufundi, Biblia, Historia, na mengineyo kwa kusikiliza vipindi mbalimbali vya sauti (audio).

Hatua 6: Uliza maswali mawili ya tafakuri kila mara, mfano unapokutana na mtu fulani: swali la kwanza ni "Je ni jambo gani nimefanya vyema?" swali la pili "ni kitu gani naweza kufanya tofauti?" Swali la kwanza linakulazimisha kufikiri kwa kina na kukumbuka mambo yote sahihi uliyoyafanya mara ya mwisho ulipokutana na mtu fulani, katika mkutano, ulipofanya uwasilishaji ama masomo ya Biblia: hata kama hayakufanikiwa. Swali la pili linakulazimisha kufikiri juu ya njia mbalimbali tofauti unazoweza kutumia kuongeza ufanisi katika mazingira yaleyale. Andika mawazo haya mahali fulani pia. Njia hii ndiyo ya haraka na zoezi la muhimu zaidi katika ukuaji binafsi na kuendelea kwa mtu.

Hatua ya 7: Mchukulie kila mtu unayekutana naye kama lulu ama thamani kubwa ya fecha, Mchukulie kama raia mtarajiwa wa mbinguni: kote nyumbani na shuleni au ofisini, Unapotembelea watu nyumbani kwao na kila unayekutana naye. Unapowachukulia watu kuwa wa muhimu na wa thamani, watarejesha fadhila kwa kukuchukulia kama mtu wa thamani pia. Hata watu wengine unaokutana nao mtandaoni ukipata nafasi ya kuwajua waweza kuwa msaada mkubwa kwako kwa kujiendeleza. Anza kwa watu wa nyumbani kwako unapoamka asubuhi, washukuru, kuwa na mtizamo sahihi utajikuta una amani na furaha siku nzima. 85% ya mafanikio yako yanategemea mahusiano yako na watu, usiwe mtu wa kukasirika kasirika (mudi mudi!). Mpende jirani yako kama nafsi yako! Ndiyo amri ya pili. Ya kwanza ni mpende BWANA MUNGU wako kwa ROHO yako yote, kwa moyo wako wote, nguvu zako zote, na akili zako zote.
Mshukuru Mungu uendapo kulala na panga siku yako itakavyokuwa usiamke bila

mipango na kuelea elea tu hewani siku nzima ukienda kama meli isiyokuwa na nanga-soma kitabu “The atomic Habits of Successful People”

*Kabla ya kuondoka nyumbani kwa ajili ya kazi, familia yote inapaswa kuitwa pamoja; na baba, au mama wakati baba hayupo, wanapaswa kumsihi MUNGU kwa bidii ili awahifadhi kwa siku nzima. Njoo kwa unyenyekevu, na moyo ulioshehení wema, upendo na upole, na kwa hisia moyoni za majaribu na hatari zilizo mbele yako na watoto wako; kwa imani uwafunge madhabahuni, na kuomba kwa bidii na moyo wote kwa ajili ya utunzaji wa Bwana. Malaika wanaohudumu watawalinda watoto ambao wamewekwa wakfu kwa MUNGU kwa namna hiyo. Kila Nyumba iwe Nyumba ya Maombi—Kama kumewahi kuwa na wakati ambapo kila nyumba inapaswa kuwa nyumba ya maombi ni sasa.

---

Orodhesha tabia tatu za ufanisi na uzielezee. Kuja kwa Yesu mara ya pili ni tumaini ambalo watu wamekuwa nalo kwa miaka mingi, Je, unajitayarishaje kwa ujio Wake Yesu?

**SIKU YA 366**
**(Desemba 31)**

**Yn 17:3**



Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.

Mbinu za kusoma Maandiko Matakatifu:

1. Kusoma kwa sura na baadaye uichambue hiyo sura: Leo Soma Sura ya 17 na chambua

a. Wazo kuu ni nini? Mfano, e,g wazo kuu la Mwanzo moja ni uumbaji.
b. Somo linaloongoza ni lipi? (leading subject)
c. Fungu maalumu ni lipi katika sura hiyo?
d. Fungu unalolipenda kupita yote ni lipi?
e. Watu gani wanahusika sura hii?
f. Sura hii yaonyesha nini kuhusu Bwana?
g. Ni mfano gani wa muhimu kufuata katika maisha yangu leo? (personalize)
h. Je, kuna ahadi gani kwangu katika sura hii?
i. Je, Kuna jukumu, linalobidi nilitelekeleze kwa mtu fulani baada ya kusoma sura hii?
j. Mambo ya kuombea katika sura hii ni yapi?

Kusoma kwa paragrafu.

2. Kusoma kutokana somo au kichwa au mada (subject). Mf: mifano ya Yesu, maombi ya watu mbali mbali, miujiza, visa, na mazungumzo ya watu waliotajwa.
3. Kusoma kwa mafungu; mfano, Warumi 8:28
4. Kusoma kutokana na maneno, agano la kale kwenye Kiebrania lina maneno 8,674 na agano jipya maneno 6,000 hivi.
5. Kusoma kutokana na maombi ya watu. Agano la kale lina sala themanini na tatu na jipya sala arobaini na tisa.
6. Kusoma kutokana na historia ya maisha ya watu. Mfano, Mfalme Daudi au Yusufu, Mume wa Mariamu, twaona biblia ina Zacharia thelathini kwenye Agano laKkale, na kumi na watano katika agano jipya. Yona wako saba na Yakobo watano.
7. Kusoma kutokana na unabii uliotimia; mfano, unabii wa Daniel 2 au 7.
8. Kusoma mafungu yote yenye Kristo katika Biblia yote. Luka 24:27, yasema

maandiko na manabii yamweleza Yeye.

9. Kusoma kitabu kimoja; mfano, Mathayo yote, kwa siku moja na kuitafakari.
10. kusoma kwa maswali na majibu.
11. Kusoma kwa kunakili kitabu kizima cha Biblia ukiendelea kutafakari.

*Bwana Hakubali Ibada ya Familia Ambayo Imekuwa ya mazoea (ni mfano tu au desturi) —Mara nyingi ibada ya asubuhi na jioni ni zaidi kidogo ya mazoea, ni duni (inaboesha), inachosha kwa semie za kujirudiarudia, ambamo roho ya shukrani au hisia ya uhitaji wao Mungu hazidhiriki. Bwana hakubali huduma kama hiyo. Lakini maombi ya moyo mnyenyekevu na roho iliyopondeka Yeye hatayadharau/ hatayapuuza. Kufungua mioyo yetu kwa Baba yetu wa mbinguni, kutambua na kukiri utegemezi wetu wote Kwake, kutanabaisha mahitaji yetu, ibada ya upendo wenye shukrani—ndiyo ombi la Kweli.

---

Taja aina mbili za kusoma Biblia ambazo wewe unapanga kuzitumia. Je, una Biblia? Kama huna ni nini kinafanya usiwe na Biblia

**Rejelea**

1. Biblia ya Kiswahili, Swahili Word Project, Union Version, and Bible Society of Tanzania. Dodoma Tanzania. 1997.

2. Arthur S Maxwell. *The Bible Story*- 10 Volumes. Review and Herald. Hagerstown, Maryland, USA. 1954.

3. Jesse Lyman Hurlbut, *Bedtime Bible Story Book*, 1989. Barbour and Company, inc. Florida, USA.

4. George W Knight. *The layman's BIBLE handbook*. Description of 66 books. 2003. Barbour Press.

5. RevivalandReformation.org Bible Blog.

6. Jack Blanco. Clear Word Devotional Bible.Year and printing press

7. Revivalandreformation.org blogu

8. Kuzaa na Kulea na Grace Momadi-Masaka

9. Masomo ya Biblia na Msafiri Mtenzi

10. Character building Stories. Inter-American Division Publishing. Association. 4 volumes.
Review and Herald Publication association, Hagerstown, Maryland. 2000.

11. George Knight. *Turn your Eyes Upon Jesus*. 2013. Review and Herald
12. GotQuestions. Org By Michael Houdmann

13. *Messiah: The Simplified Desire of Ages*. Jerry D. Thomas.2002. pacific Press. Nampa Idaho, USA

14. My Bible First.org . Website.

**ARIHISI**

**NINI KIPO NDANI YA BIBLIA:** Mungu amejifunua kwa watu Wake, ni historia ya kile Mungu alichokifanya na kusema na watu wake.

**Kwa nini Biblia ni muhimu:**
Ni pumzi ya Neno la Mungu, inatufundisha Mungu alivyo, inatuonesha mema na maovu, inatufundisha jinsi ya kuishi na watu, inatuonesha upendo wa Mungu hata kufa, inatufundisha jinsi ya kuomba toba, kutusaidia tusiogope, kutusaidia tuzungumze na Mungu, kufanya tufanye uamuzi, inatuonesha mambo ya mbinguni na jinsi ya kufika huko, na jinsi ya kuwa na furaha na shukrani.

Biblia si kitabu tu cha kujifunza mambo bali ni ramani ya jinsi ya kuishi,na kufanya uchaguzi kwa yale yanayotufaa na kusaidia kuleta furaha hapa duniani na katika umilele. Inatuonesha jinsi tunavyoweza kuwa rafiki wa Mungu na kwamba Mungu anatupenda sana.

Nimetoka wapi?
Mungu ni nani na anafananaje
Jambo lipi ni jema au zuri la mtu kufanya
Je, nawezaje kupata marafiki, na kuwatunza- kwa nini Yesu alikufa msalabani?
Nawezaje kusamehewa nikifanya dhambi au makosa?
Nifanyeje nikiwa na hofu, woga au wasiwasi? Nazungumzaje na Mungu?
Mbinguni ni wapi na ninawezaje kupata uzima wa milele?
Nawezaje kuwa mtu mwenye furaha na shukrani?

***Mafundisho machache ya kuangalia kwa haraka-kutokana na somo***.

***Ahadi za Mungu***
Ibrahimu-Ahadi za kuwa na watoto kama nyota-Mwanzo
Mwizi msalabani-Aliahidiwa uzima wa milele

***Amri za Mungu***
Mlima wa Sinai-zilitolewa Amri Kumi-Kutoka
Neno la Mungu- Amri, maagizo, shuhuda, Maandiko-Zaburi 119
Mkazo wa Amri- Mlima wa Baraka-Mathayo

***Dhambi na matokeo yake*** Dhambi ya kwanza-Mwanzo Matokeo ya dhambi-Mwanzo
Kaini-Kutiwa chapa baada ya dhambi-Mwanzo

Gharika-Uovu mkuu siku zile-Mwanzo
Sodoma-Kuunguzwa na moto kwa uovu-Mwanzo
Haruni- Kutengeneza ndama-Kutoka
Waamuzi-Siku ambazo watu walifanya waliyoona mema-Waamuzi
Akani-Kuiba vitu vilivyokuwa wakfu-Hesabu
Daudi-Kuchukua mke wa mtu-Samweli

Ahabu-uovu wa kuchukua shamba la Nabothi-Wafalme
Manase Mfalme mwovu-Wafalme
Belshaza-Maandishi ukutani
Mateka-Wayahudi wachukuliwa Babeli na Nebukadreza-Yeremia
Sauli-Kwenda kwa mchawi wa Endori

***Gharika na athari zake***
Nuhu na gharika-Mwanzo
Mnara wa Babeli-Watu wataka kujua maji yametoka wapi-Mwanzo

***Imani***
Ibrahimu-Akatoka Uru na kuelekea Kanaani-Mwanzo Ibrahimu-Awa tayari kumtoa mwanawe sadaka-Mwanzo Yeriko-Ukuta waanguka-Yoshua
Mafuta-Ambayo hayakupunguka kwa mjane wa Sarepta
Mafuta-Yajaa kwenye vyombo vya mjane
Kwaya-yashinda vita chini ya Mfalme Yehoshafati Shamu-Kuvuka bahari ya Shamu Pakavu-Kutoka Yordani-Kuvuka mto Yordani pakavu-Yoshua
Uponyaji wa Yesu kwa watu mbali mbali-Mwanamke aliyegusa pindo la vazi

***Uaminifu***
Yusufu-Akiwa nyumbani, gerezani na hata ikulu-Mwanzo
Bezaleli-Mjenzi wa hekalu-Kutoka
Huramu-Mkataji wa shaba hekalu la Sulemani
Talanta-Mfano wa Yesu wa uaminifu

***Kuamua kufanya mambo haraka bila kufikiri***
Yeftha mwamuzi-aliamua kutoa kafara kitakachomlaki-Waamuzi
Musa-Kumwua Mmisri -Kutoka

***Kuchagua kwa hekima***
Esau-auzwa kwa chakula na uchaguzi mbaya-Mwanzo
Sulemani-Aomba moyo wa hekima-Wafalme
Mariamu-Achagua fungu jema kulinganisha na Martha

***Kujisifia-si kitu chema***
Hezekia-ajisifia badala ya kushuhudia-Isaya
Nebukadreza-arukwa na akili kwa kujisifia-Danieli

***Kujitoa kwa Mungu***
Ruthu –Mmoabi ajitoa kwa Mungu-Ruthu
Mama Samweli-ajitoa kwa Mungu na kumpa mwanawe-Samweli Yosia-Mfalme ajitoa kujenga hekalu na kuleta matengenezo-Wafalme Eliya –Ajitoa kumtetea Mungu mlima Karmeli-Wafalme
Daudi- ajitoa kwa kuandaa sadaka ya kujenga hekalu-Wafalme?

***Kujitoa wakfu***
Wana wa Haruni wawekwa wakfu-Walawi

Hezekia-awaambia watu walitakase hekalu na kuliweka wakfu-Wafalme
Yesu-aiweka wakfu mikate na kulisha watu 5000-Mathayo

***Kukata tamaa***
Yohana- Alikata tamaa Patmo, akatiwa moyo-Ufunuo

***Kulea na kufundisha watoto***
Musa-Malezi bora ni muhimu kwa mtoto ili ampende Mungu-Kutoka

***Kusamehe***
Petro-aambiwa asamehe kama Mungu
Mateso ya Yesu-Yesu asamehe watesi-Mathayo, Luka na Marko

***Kutembea na Mungu***
Henoko-atwaliwa mbinguni-Mwanzo
Eliya-atwaliwa na Mungu

***Kutokuwa na shukurani***
Wakoma tisa-hawakurudi kusema asante
Absalomu-Kutoshukuru kuwa alisamehewa

***Kuongoka***
Nikodemo- Mgeni wa usiku aongoka-Yohana Mwanamke Msamaria- Kisimani Sikari-Yohana Zakayo-Mwenye tamaa awa mkarimu-Luka
Paulo- Adui wa Yesu awa shujaa wa Yesu-Matendo

***Kuoa wasioamini***
Ezra-Awaambia warudishe wake wageni-Ezra

***Kushuhudia wengine***
Ibrahimu-Maisha yake alipoishi-Mwanzo
Malkia wa Sheba-Alikuja kuona ukuu wa Mungu
Mlima wa Karmeli-Watu wajua ni nani Mungu wa kweli- Mfanyakazi wa Naamani-Amshuhudia tajiri wake Walioponywa na Yesu-washuhudia-Vitabu vya Injili Efeso-vitabu vya uchawi vyachomwa-Matendo
Saulo- abadilika kuwa Paulo-Matendo
Uje Makedonia-Paulo aona ndoto-Matendo

***Kupenda kutoa udhuru***
Sitakuja arusini-Shuguli ni nyingi, walitoa udhuru

***Kutoamua-Hatari zake***
Feliki, Agripa na Festo-walikosa mbingu kwa sentimeta chache-Matendo

***Kutokata tamaa***
Paulo-Alivipiga vitu vizuri na mwendo akamaliza-Timotheo
Nehemia, Ezra, Zerubabeli-ujenzi wa hekalu na mji-Nehemia/Ezra

***Kutotii***
Sauli-Mfalme asiyetii na matokeo yake-Samweli
Uza-Ashika sanduku na kufa papo hapo
Daudi-Ahesabu watu na kupewa adhabu-Mambo ya Nyakati
Sulemani-Atii wake zake kuliko Mungu, akaabudu miungu
Ufalme-Wagawanyika kwa kutotii - Wafalme
Hekalu la Sulemani- laibiwa na mfalme Shishaki wa Misri-Wafalme
Nabii- Auawa na simba kwa kutotii
Zimri, Omri-Na  Wafalme wengi wasiotii-Wafalme
Yona-Aliwa na samaki kwa kutotii-Yona
Maandiko - Ni muhimu, kila mtoto ayasome
Yesu afundisha marabi Maandiko akiwa mtoto. Luka
Waberoya walichunguza Maandiko-Matendo
Kleopa-Njiani Yesu aliwaelezea-Luka
Towashi-Mkushi alikuwa akisoma Maandiko-Matendo

***Mbinguni***
Mbingu mpya na nchi mpya-Mji wa Yerusalemu-Ufunuo

***Maisha ya Yesu***
Kuzaliwa, kufufuka, kufa, Mateso, kupaa-vitabu vya Injili

***Malaika***
Kisa cha Samsoni - Waamuzi
Usiku na simba-Kisa cha Danieli na Simba-Danieli
Habari njema –Malaika waimba kuzaliwa kwa Yesu
Mama wawili-Mariamu na Elizabethi walipochukua mimba
Kwaya ya malaika-Kuzaliwa kwa Yesu
Yusufu- Aambiwa amchukue mtoto Yesu Misri
Petro- Atolewa gerezani na malaika-Matendo
Paulo-Malaika amweleza hakuna atakayepotea-Matendo
Yesu-afarijiwa na malaika bustani ya Gethsemane-Yohana

***Mbinguni ni mahali halisi***
Makao-Mungu ametuandalia makao mbinguni-Yohana, Mathayo
Mbinguni-Mungu ameandaa mji wa ajabu-Ufunuo

***Maombi***
Sala kuu-Yesu awafundisha wanafunzi kuomba-Mathayo
Sala ya Yesu Gethsemane-Yohana
Farisayo na Mtoza ushuru-maombi mawili-Luka Sulemani-Ombi la kuweka wakfu hekalu-Wafalme Eliya- aomba mvua mara saba-Wafalme
Nehemia-Amwomba Mungu amsaidie-Nehemia
Yakobo-aomba na kuteguliwa mguu-Mwanzo

***Rehema za Mungu***
Ngazi ya Yakobo-Malaika wakishuka na kupanda-Mwanzo

Mtango wa Yona-Uliokufa kwa siku moja-Yona
Kufa msalabani-Na upendo Wake-Biblia nzima

***Kutubu***
Daudi- Maungamo yake-Zaburi na Wafalme
Kijana mpotevu-Alirudi na kuungama-Luka

***Roho Mtakatifu***
Karama-Mungu ameahidi-Matendo

***Sabato***
Siku ya kukumbuka-Mwanzo
Mana-Haikuanguka Sabato-Kutoka
Mambo ya kufanya siku ya Sabato-vitabu vya injili
Yesu – Aliendа hekaluni, alipumzika kaburini -Vitabu vya injili

***Siri za furaha***
Mlima wa baraka-Soma mafundisho yake Mathayo 5-7

***Tamaa***
Ahabu-Atamani shamba ya mizabibu la Nabothi
Gehazi-Mtumishi wa nabii apata tamaa ya vitu vya Naamani-Wafalme

***Ubatizo***
Yohana mbatizaji-Mto Yordani-Mathayo
Towashi mkushi-Abatizwa-Matendo

***Ulalamishi***
Wana wa Israeli-walilalamika kwa chakula, maji, na yote-vitabu vya Musa
Ndugu za Musa-Kwa nini 'Mungu amtokee Musa' na si wao
Kanaani-safari ilichukua miaka 40 badala ya wiki mbili-Kutoka

***Ushujaa***
Mashujaa wa Daudi 30
Daudi shujaa asimikwa-Shujaa aliyepigana na dubu/simba-Samweli
Selofeadi-Wasichana tano mashujaa wabadilisha historia
Yonathani-mtoto wa mfalme shujaa ashinda vita Daudi aokoa watu waliotekwa na Waamaleki Zerubabeli-Atiwa ushujaa awe na nguvu
Nehemia-awatia watu moyo wasiogope vitisho-Nehemia
Esta-Afanya maamuzi ya ushujaa kwenda kumwona mfalme-Esta
Paulo na Sila-Waimba gerezani kwa ushujaa

***Uongo au Ulaghai***
Uongo-Unaumiza, ulimtelea maumivu mengi Yakobo-Mwanzo
Mkate wenye Fangasi

***Uongozi wa Mungu/Miujiza***

Wanyama-Waingia kwenye safina wenyewe-Mwanzo Miujiza yote waliyotendwa
Wana wa Israeli-Biblia Fimbo ya Haruni-Kutoa maua-Walawi
Yoshua-Akutana na Kamanda wa Majeshi ya BWANA-Yoshua
Gideoni-Ishara ya manyoya ya kondoo-Waamuzi Samweli-Kuongozwa kuchagua mfalme-Samweli Esta- awa Malkia-Esta
Mamajusi-Waongozwa kwenda kumwona Yesu-Mathayo? Yesu -Aenda Misri na wazazi-Mathayo
Nebukadreza-Asahau ndoto yake-Danieli
Yebusi yawa Yerusalemu
Kurudi toka Babeli-chini ya uongozi wa Ezra, Zerubabeli na Yoshua-Ezra

***Ukarimu***

Sadaka-wana wa Israeli walitoa mpaka wakaambiwa imetosha
Barnaba-Na wengine watoa nyumba zao
Tabia ya mbinguni-wale wanaomtendea Yesu mema-Mathayo 25

***Unyenyekevu***

Salome Zebedayo-ataka watoto wapate cheo-Luka Yesu aosha miguu-Unyenyekevu ni muhimu. Mfarisayo na mtoza ushuru-hekaluni wakiomba

***Upendeleo***

Petro agundua Mungu hana upendeleo kwa Kornelio-Matendo
Yakobo-Na mitume waandika barua kwa wa-Mataifa-Matendo

***Upendo wa Mungu na Ukuu***

Mungu- Kumtuma Mwanawe-Vitabu vya Injili
Yesu-Aishi na watu, kuwaponya na kuwasaidia-Vitabu vya Injili Mifano ya Yesu-Mwana mpotevu, Kondoo aliyepotea-Vitabu vya Injili Mungu ni upendo-Barua za Yohana
Karamu ya mwisho
Yesu kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu

***Utunzaji wa Mungu***

Nuhu-Mungu amtunza kwenye safina –Mwanzo Yusufu-katika shida zake zote utumwani-Mwanzo Musa-Ndani ya kikapu-Kutoka
Balaamu-Punda azungumza naye-Hesabu
Daudi-kuokoka mikononi mwa Sauli-Samweli, Wafalme
Eliya-Alishwa na kunguru-Wafalme
Elisha-alindwa na jeshi
Yosia-afichwa kwenye hekalu
Mpwa wa Paulo-Alimsaidia Paulo kuokoka dhidi ya watu 470-Matendo
Hamani-Hila zake zashindwa kuua Wayahudi-Esta Mordekai-Kugundua watu waliotaka kumwua mfalme-Esta Yesu-Kuzaliwa Kwake na maisha Yake-Vitabu vya Injili

***Uwezo wa Mungu***
Kutembea juu ya maji-Mathayo
Yordani na Shamu-Kuvuka mto pakiwa pakavu
Yoshua-Jua lasimama-Yoshua
Shadraki, Meshaki, na Abednego-Kwenye moto-Danieli
Shoka laelea majini-Wafalme?
Jua larudi nyuma-Wakati wa Hezekia
Arusi ya Kana-Yohana
Miujiza yote katika maandiko

***Roho ya Urafiki***
Yonathani na Daudi –Wafalme
Isaka-Aendelea kuchimba visima

***Mungu Mwumbaji***
Mungu aliumba mbingu, maisha, dunia na vyote-Mwanzo

***Malipo ya wivu***
Hamani-Kutaka kuua Wayahudi-Esta
Yusufu –Kuuzwa na nduguze utumwani-Mwanzo
Mikali-Kuweka sanamu ya mtu kwenye kitanda-Samweli
Daudi-Kuchukua Jambia la Goliathi

***Mpango wa Wokovu***
Pasaka-Damu kwenye mlango-Kutoka Nyoka jangwani-Musa alimwinua
Rahabu-kamba nyekundu-Hesabu
Yesu-Mwanakondoo wa Mungu-Vitabu vya Injili

***Wema hauozi***
Rebeka-Msichana aliyesaidia kunywesha ngamia-Mwanzo
Raheli-Msichana aliyemsaidia Yakobo-Mwanzo
Mshunami-amfadhili Elisha, naye asaidiwa
Ebed-meleki mkushi-Amsaidia Yeremia-Yeremia
Mefiboshethi-asaidiwa na Daudi kwa wema wa Yonathani

***Wito toka kwa Mungu***
Musa- aitwa jangwani kumtumikia Mungu-Kutoka Samsoni- Mnazarayo aitwa amtumikie Mungu-Waamuzi Samweli-aitwa kumtumikia Mungu-Samweli
Eliya- Alisikia sauti ndogo ya Mungu-Wafalme
Isaya-Aitwa kumtumikia Mungu
Yeremia-Aitwa kuwa nabii-Yeremia
Yesu-aitwa kuanza huduma-Mathayo, Luka Mitume waitwa-Mathayo, Yohana, Luka Mitume-waitwa kuvua watu
Malaika-waita watu wamche Mungu-Ufunuo

***Yesu Anakuja tena***
Dalili za kuja kwa Yesu-Mathayo
Jinsi Yesu atakavyorudi-Vitabu vya Injili
Jinsi Yesu atakavyokuja-Ufunuo

***Unabii Watimia***
Sanamu ya ajabu-Falme zitakazotawala dunia-Danieli Wanyama wa ajabu-Falme zitakazotawala dunia-Danieli Yesu-Kuzaliwa Kwake kulitimiza unabii-Injili

***Uponyaji wa Yesu***
Miujiza yote ya Yesu-vitabu vya Injili

***Utii na uaminifu***
Nuhu-kujenga safina-Mwanzo
Ibrahimu-Baba wa imani- Mwanzo
Yusufu-Maisha ya kumtegemea Mungu-Mwanzo
Vijana Babeli-Danieli, Mishaeli, Azaria, Hanania-Danieli
Ayubu-uaminifu wake kwa Mungu-Ayubu Dura-Vijana watatu wa Babeli-Danieli
Washindi-Watapata thawabu-Danieli
Musa-Kupiga mwamba mara mbili Meriba-Kutoka
Sauli-Utii ni bora kuliko dhabihu
Farao-Kufanya moyo wake kuwa mgumu-Kutoka

***Zaka***
Ibrahimu- alimpatia Melkizekedi-Mwanzo
Madirisha ya mbinguni-Mungu atafungua-Malaki

**MADA SIKU KWA SIKU ZA SOMA VISA vya BIBLIA Zaidi ya 407 kwa**

**Mwaka mmoja (siku 366)**

1. Mwanzo au Uumbaji - Mwanzo
2. Kuumbwa kwa Mwanadamu- Mwanzo 1 & 2 Takribani mwaka 4000
3. Siku ya Saba na ya Mapumziko kwa Binadamu Mwanzo 2
4. Siku ya Saba na ya Mapumziko kwa Binadamu - Mwanzo 2
5. Shetani Aanguka Toka Mbinguni - Ufunuo 12, Ezekieli 28, Isaya 14, Yohana 3:14-20
6. Adhabu ya Uasi - Mwanzo 3
7. Mtoto wa Kwanza na Kifo cha Kwanza - Mwanzo 4
8. Maisha ya Henoko - Mwanzo 5-8
9. Nuhu, Safina, na Gharika - Mwanzo 6-8 takribani 2348KK
10. Mnara wa Babeli - Mwanzo 9-11
11. Abramu - Baba wa Wenye Imani - Mwanzo 13-14 takribani Mwaka 2000KK
12. Kuzaliwa kwa Ishmaeli na Ahadi ya Kuzaliwa kwa Isaka - Mwanzo 15-17
13. Ibrahimu Azungumza na Mungu na Mvua ya Moto - Mwanzo 18 na 19
14. Kuzaliwa kwa Isaka - Mwanzo 20 na 21
15. Mtihani Mkubwa kwa Ibrahimu - Mwanzo 22-24
16. Mke kwa Ajili ya Isaka - Mwanzo 24
17. Ugomvi wa Mapacha na Uzaliwa wa Kwanza - Mwanzo 25
18. Yakobo Achukua Baraka za Esau - Mwanzo 27 na 28
19. Familia ya Yakobo - Mwanzo 29-31
20. Mweleka Wakati wa Usiku - Mwanzo 31-33
21. Yusufu na Ndugu Zake - Mwanzo 35-39
22. Yusufu Atoka Jela - Mwanzo 40-41
23. Wana wa Yakobo Waenda Kununua Nafaka - Mwanzo 42 –43
24. Yakobo Akutana na Yusufu - Mwanzo 44 na 45
25. Familia ya Yakobo Yaenda Misri - Mwanzo 45 na 46
26. Yakobo Atoa Baraka kwa Wanawe - Mwanzo 49 na 50
27. Kuzaliwa kwa Musa - Kutoka 1 na 2
28. Musa na Kijiti Kilichowaka Moto - Kutoka 3 na 4
29. Mbele ya Farao - Kutoka 5-7, Takribani mwaka 1400KK
30. Mapigo ya Misri - Kutoka 8-11
31. Pasaka ya Kwanza - Kutoka 12 na 13
32. Kuvuka Bahari ya Shamu - Kutoka 14
33. Maji Machungu na Mkate wa Mana - Kutoka 16.
34. Maji ya Meriba na Kugawanya Uongozi- Kutoka 17 na 18
35. Amri Kumi Katika Mlima wa Sinai (Horebu) - Kutoka 19 na 20
36. Sheria na Hukumu - Kutoka 20 na 21
37. 37“Wanijengee Patakatifu” - Kutoka 24-27
38. Dhambi ya Kuabudu Ndama wa Dhahabu - Kutoka 32 na 33
39. Musa Aenda Tena Mlimani - Kutoka 34 na 35
40. Sababu za Kuwa na Patakatifu - Kutoka 25, Mambo ya Walawi 16 na 22
41. Kuwaweka Wakfu Makuhani - Kutoka 28, 27, 39 na 28
42. Huduma za Patakatifu - Kutoka 27, 35-40 na Mambo ya Walawi 1 na 8

na Hesabu 10

43. Utakatifu wa Huduma za Makuhani – Mambo ya Walawi 1- 10
44. Siku ya Upatanisho – Mambo ya Walawi 16
45. Najisi na Visivyo Najisi - Walawi 11-19
46. Mungu na Watu Wake Wanaolalamika - Mambo ya Walawi 26, Hesabu 1 na 7 na 11
47. Ndugu wa Musa na Uasi - Hesabu 12 na 16
48. Wapelelezi 12 - Hesabu 13-15
49. Maji ya Meriba Yamfanya Musa Asiingie Kanaani - Hesabu 20
50. Safarini na Changamoto zaendelea - Hesabu 21-26
51. Matoleo na Sikukuu na Kuhesabiwa kwa Waisraeli - Hesabu 26-31
52. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati
53. Kifo cha Musa - Hesabu 27 na Kumbukumbu la Torati 31-34
54. Rahabu na Kamba Nyekundu - Yoshua 1-3
55. Kuvuka Mto Yordani kwa miujiza - Yoshua 3-5
56. Yoshua Akutana na Kamanda wa Majeshi - Yoshua 5 na 6
57. Dhambi ya Akani ya tamaa- Yoshua 7
58. Yoshua Adanganywa na Wagibeoni na Jua Lasimama - Yoshua10-21
59. Siku za Mwisho za Yoshua - Yoshua 21-24
60. Waamuzi - Yoshua 24 na Waamuzi 1
61. Waamuzi wa Kwanza na Uasi wa Israeli - Waamuzi 3-6
62. Gideoni na Watu 300 - Waamuzi 6-9
63. Yeftha na Nadhiri ya Kafara - Waamuzi 9-13
64. Samsoni Mnadhiri wa Mungu Waamuzi
65. 13 na 14
66. Kitendawili cha Samsoni - Waamuzi 14-16
67. Mwisho wa Samsoni - Waamuzi 16
68. Hekalu la Sanamu la Mika - Waamuzi 17 na 18
69. Uovu Katika Israeli - Waamuzi 19-21 (takribani 1400-1000 KK)
70. Naomi Arejea Nyumbani - Ruthu 1
71. Boazi Amwoa Ruthu - Ruthu 2-4
72. Mtoto Samweli – 1 Samweli 1-3
73. Mtoto Samweli Akiwa Hekaluni – 1 Samweli 2-3
74. Wafilisti Wachukua Sanduku la Agano (Ikabodi) - 1 Samweli 4-7
75. Samweli, Mwamuzi wa Mwisho wa Israeli - 1 Samweli 7-9
76. Sauli Atiwa Mafuta Kuwa Mfalme - 1 Samweli 9-12
77. Sauli Afanya Dhambi kwa Kufanya Huduma ya Kuhani – 1 Samweli 13-14
78. Mungu Ajuta Juu ya Sauli - 1 Samweli 15-16
79. Daudi Achaguliwa Kuwa Mfalme - 1 Samweli 16-17, Takribani mwaka 1000KK
80. Daudi na Goliathi jitu- 1 Samweli 17
81. Urafiki mkubwa wa Daudi na Yonathani - 1 Samweli 18-20
82. Sauli Aua Makuhani 85 watakatifu na familia zao - 1 Samweli 20-22
83. Abiathari Akimbilia kwa Daudi - 1 Samweli 22-24
84. Daudi, Nabali na Abigaili - 1 Samweli 25
85. Sauli Amwinda Tena Daudi - 1 Samweli 26-28

86. Mchawi wa Endori - 1 Samweli 29-30
87. Madanganyo ya Shetani eti mtu akifa unaweza kuwasiliana naye - 1 Samweli 29 na 30
88. Kifo cha Sauli - 1 Samweli 30-2 Samweli 1-3, 1 Mambo ya Nyakati 10
89. Daudi Atawala Hebroni na Israeli Yote - 2 Samweli 3-5
90. Kurudisha Hisani Kupitia kwa Mefiboshethi - 2 Samweli 8-10
91. Dhambi Kubwa ya Daudi - 2 Samweli 11
92. Adhabu ya Daudi - 2 Samweli 12
93. Toba ya dhati ya Daudi - Zaburi 32 na 51
94. Uovu Nyumbani mwa Daudi - 2 Samweli 12-13
95. Absalomu mwana wa Daudi na Yoabu binamuye - 2 Samweli 14
96. Uasi wa Absalomu - 2 Samweli 15
97. Absalomu Afanya Vita na Babaye - 2 Samweli 15-18
98. Absalomu Auawa - 2 Samweli 18-19
99. Daudi Arejea Katika Ufalme - 2 Samweli 19-21
100. Mashujaa wa Daudi - 2 Samweli 22-23
101. Daudi Awahesabu Israeli - 2 Samweli 24 na 1 Mambo ya Nyakati 21
102. Kutawazwa kwa Sulemani - 1 Wafalme 1
103. Zaburi - Nyimbo na Ibada - Zaburi 1-150
104. Sulemani na Maagizo ya Baba Yake - 1 Wafalme 2-3
105. BWANA Amtokea Sulemani - 2 Wafalme 3 na 2 Mambo ya Nyakati 1
106. Maneno ya Hekima – Mithali
107. Mithali na Mhubiri
108. Mithali na Mhubiri
109. Kujenga Hekalu - 1 Wafalme 5 na 2 Mambo ya Nyakati 1, 3
110. Ujenzi wa Hekalu Wakamilika - 1 Wafalme 6-8
111. Hekalu Lawekwa Wakfu - 1 Wafalme 8-9 na 2 Mambo ya Nyakati 4-6
112. Jibu la BWANA kwa Sulemani - 1 Wafalme na 2 Mambo ya Nyakati 7 na 9
113. Wimbo Ulio Bora au Wimbo wa Sulemani
114. Sulemani Amwacha Mungu - 1 Wafalme 11
115. Rehoboamu Mwana wa Sulemani Arithi Yuda - 1 Wafalme 12 na 2 Mambo ya Nyakati 9-11
116. Ufalme wa Israeli Wagawanyika - 1 Wafalme 12 na 1 Mambo ya Nyakati 10
117. Mkono wa Yeroboamu Wapooza - 1 Wafalme 13 na 2 Mambo ya Nyakati 13
118. Wafalme wa Yuda na Israeli - 1 Wafalme 14, 15 na 2 Mambo ya Nyakati 10
119. Wafalme na Nabii Eliya-Mtishbi - 1 Wafalme 15-17 na 2 Mambo ya Nyakati 16
120. Mwana wa Mjane wa Sarepta Afufuliwa - 1 Wafalme 17
121. Manabii wa Baali na Ashera Mlimani Karmeli - 1 Wafalme 18
122. Eliya Apungukiwa Ujasiri na Kukimbia - 1 Wafalme 19
123. Eliya Amtia Mafuta Mrithi Wake - 1 Wafalme 20
124. Shamba la Nabothi - 1 Wafalme 21
125. Siku za Mwisho za Ahabu - 1 Wafalme 22 na 2 Mambo ya Nyakati 18

126. Yehoshafati, Ahazia na Eliya - 1 Wafalme 22, 2 Wafalme 1 na 2 Mambo ya Nyakati 17-19
127. Nabii Eliya Atwaliwa Mbinguni - 2 Wafalme 1 na 2
128. Watoto Wakorofi Waadhibiwa - 2 Wafalme 2-3
129. Mwanamke Mjane na Mafuta na Mwanamke Mshunemu - 2 Wafalme 4-6
130. Chakula Chenye Sumu na Shoka Lililozama - 2 Wafalme 4-6
131. Jemedari Naamani na Mjakazi Mtumwa - 2 Wafalme 5
132. Ukoma wa Naamani Wahamia kwa Gehazi - 2 Wafalme 5
133. Magari ya Moto - 2 Wafalme 6
134. BWANA Awapigania Israeli - 2 Wafalme 6-7
135. Hazaeli Awa Mfalme wa Shamu - 2 Wafalme 8
136. Utawala wa Yehu - 2 Wafalme 9-10
137. Yoashi-Mfalme Mtoto - 2 Wafalme 11-13; 2 Mambo ya Nyakati 24
138. Kwaya Iliyoshinda Vita - 2 Wafalme 19-20
139. Miaka ya Uovu wa Wafalme - 2 Wafalme 14-15 na 2 Mambo ya Nyakati 25- 28
140. Wafalme Zaidi - 2 Wafalme 15 na 2 Mambo ya Nyakati 28
141. Makabila 10 ya Israeli Yalivyopotea - 2 Wafalme 15-17
142. Mfalme Hezekia - 2 Wafalme 18-19; 2 Mambo ya Nyakati 29-32; Isaya 36-37
143. Kuugua kwa Hezekia - 2 Wafalme 20; 2 Mambo ya Nyakati 29-32; Isaya 38-39
144. Mfalme Manase na Yosia - 2 Wafalme 21; 2 Mambo ya Nyakati 33
145. Yosia Afanya Matengenezo - 2 Wafalme 23; Mambo ya Nyakati 34-35
146. Ufalme wa Mwisho wa Yuda - 2 Wafalme 24-25; 2 Mambo ya Nyakati 35; Isaya 45
147. Ezra – Kuhani na mwandishi wa NENO la MUNGU
148. Ezra kuhani na Nehemia Kiongozi chini ya serikali ya uajemi
149. Nehemia – Rafiki ya Mfalme
150. Nabii Isaya
151. Ujumbe Zaidi wa Isaya
152. Ujumbe wa Yeremia Nabii - Baruku Mwandishi - 625KK
153. Ujumbe Zaidi wa Yeremia
154. Nabii Ezekieli uhamishoni Babeli Takribani mwaka 600KK
155. Ujumbe wa Ezekieli Unaendelea
156. Esta Awa Malkia wa nchi ya Uajemi iliyotawala dunia yote Takribani mwaka 478KK
157. Esta na Wayahudi Wafanya Maombi Maalumu -Esta 4-7
158. Mordekai Apandishwa Cheo na Wayahudi Wajitetea - Esta 8-10
159. Mtu wa Mungu Ayubu
160. Danieli Aenda Uhamishoni - Danieli 1
161. Somo la Chakula - Mwanzo 1:29 na Danieli 1
162. Mfalme Aota Ndoto - Danieli 2
163. Falme Zitakazotawala Dunia - Danieli 2
164. Umuhimu wa Unabii wa Danieli 2
165. Kulazimishwa Kusujudu Sanamu - Danieli 3
166. Mfalme Nebukadneza Aishi Porini - Danieli 4

167. Kiganja Chaandika Ukutani - Danieli 5
168. Danieli Atupwa Kwenye Pango la Simba - Danieli 6
169. Wanyama wa Ajabu - Danieli 7
170. Tafsiri ya Ndoto ya Danieli 7
171. Maono ya Kondoo Mume na Beberu - Danieli 8
172. Danieli Azidi Kufunuliwa Siri za Unabii - Danieli 9
173. Unabii wa Siku 2300 Wafunuliwa - Danieli 9
174. Maarifa Kuongezeka na watu kwenda huko na kule - Danieli 10-12
175. Upendo wa Mungu kwa Watu Wake – Hosea, Takribani mwaka 750KK
176. Ujumbe wa Yoeli, takribani mwaka 930KK
177. Nabii Amosi
178. Ujumbe wa Mika
179. Yona - Nabii Aliyemezwa na Samaki
180. Yona Ndani ya Samaki
181. Kujenga Hekalu – Hagai, takribani mwaka 538KK
182. Ujumbe wa Nabii Nahumu
183. Obadia siku ya BWANA
184. Habakuki – Njozi na Tumaini
185. Ujumbe wa Sefania
186. Zekaria-Ujumbe kwa Waliorejea Toka Uhamishoni
187. Malaki – Ujumbe wa Matengenezo, Takribani mwaka 420KK

**AGANO JIPYA- BAADA YA YESU AU MASIHI ISA BINMARIAMU KUZALIWA**
**YESU abadilisha historia ya dunia, Kabla ya Kristo (KK) yawa Baada ya Kristo (KK)!**
**Je, Mungu ametusahau? Watu walijiuliza baada ya ukimya**
**UPATANIFU WA VITABU VYA INJILI**

188. Je, Mungu ametusahau? Watu walijiuliza
189. Upatanifu wa Vitabu vinne vya injili. Mathayo, Marko, Luka na Yohana.
190. YESU Alikuwako siku zote, na anaendelea kuishi milele.
191. Unabii wa kuzaliwa kwa Yesu Masihi na BWANA wetu. Luka 1.
192. Kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji msafisha njia wa Masihi. Luka 1.
193. Kuzaliwa kwa Yesu Masihi na Mwana wa Mungu. Luka 2 na Mathayo 2.
194. Mamajusi kutoka mashariki wamtembelea Yesu, Mathayo 2.
195. Yesu abarikiwa hekaluni akiwa na siku 40. Luka 2.
196. Yesu hekaluni akiwa na miaka 12. Luka 2.
197. Utoto wa Yesu na Yohana mbatizaji. Luka 3, Mathayo 3 na Marko 1.
198. Yesu asimikwa kwa ubatizo mto Yordani. Yohana 3, Marko 1. Luka 3
199. Yesu anajaribiwa na Shetani nyikani. Luka 4, Mathayo 4.
200. Kuita wanafunzi wa kwanza I. Yohana 1.
201. Kuita wanafunzi wa kwanza II. Yohana 1
202. Yesu anafanya muujiza wa kwanza kwenye harusi Kana. Yohana 2.
203. Yesu apindua meza za hekalu, na kutakasa hekalu. Yohana 2.
204. Nikodemu mwanafunzi wa Yesu aliyekuja usiku. Yohana 3
205. Mwanamke Msamaria wa Sikari kisimani. Yohana 4

206. Yohana awekwa kizimbani na kuuwawa. Yohana 3. Luka 3 na Yohana 4.
207. Yesu anaanza kazi kwao Nazareti alipolelewa, Luka 4. Mathayo 4.
208. Yesu akataliwa kwao Nazareti. Luka 4
209. Wavuvi waitwa tena kuwa wanafunzi. Luka 5.
210. Mathayo aitwa awe mwanafunzi, na afanya karamu ya kuaga wenzake. Luka 5.
211. Mambo ya kufanya siku ya Sabato. Luka 6 , Luka 13 na Yohana 5.
212. Kuponya siku ya Sabato. Luka 6, 13 na Yohana 5.
213. 213 Mlango wa kuingia mbinguni ni Mwembamba. Luka 13
214. Mlima wa baraka-Heri, chumvi, taa. Luka 6, mathayo 5-7.
215. Mlima wa baraka-Sheria na kuishi maisha ya Ukristo. Luka 6. Mathayo 5-7.
216. Wana Heri au Wana furaha, au Wamebarikiwa. Mathayo 5
217. Sala ya BWANA aliyotufundisha tuombe. Mathayo 6
218. Ombeni nanyi mtapewa, Bisheni nanyi mtafunguliwa, tafuteni nanyi mtapata. Luka 11 na Mathayo 7.
219. Mtumishi wa akida wa Kirumi aponywa. Luka 7
220. Mariamu Magdalena na Marhamu ya upendo. Luka 7. Yohana 12.
221. Martha na Mariamu dada wawili waliomshughulikia Yesu. Luka 10
222. Mpazi au mpandaji mbegu, Yesu afundisha kwa mifano. Marko 3 na 4.
223. Mifano Upepo wamtii. Marko 4. Mathayo 8.
224. Mitume 12 waenda kazini. Mathayo10, Luka 9.
225. Kutuma wanafunzi 70 umishonari. Luka 10.
226. Msamaria mwema mwenye huruma. Luka 10.
227. Mungu anatuhimiza tuutafute ufalme Wake kwanza. Mathayo 10.
228. Gharama ya kuwa mwanafunzi wa Yesu. Luka 12,14 na Mathayo 10.
229. Ufalme wa mbinguni ni Lulu ya thamani, au nyavu ya samaki. Mathayo 13.
230. Mikate mitano, samaki wawili kulisha maelfu. Mathayo 14, Marko 6.
231. Petro atembea juu ya maji. Marko 6.
232. Wanafunzi wanarudi nyuma na wengine wanatoroka. Yohana 6.
233. Mwanamke aliyefumaniwa akizini. Yohana 8.
234. Kipofu aponywa. Yohana 9.
235. Kipofu aliyefumbuliwa macho atengwa ushirika. Yohana 9.
236. Mwenye pepo Gerasi. Marko 5, Mathayo 8. Luka 8.
237. Yesu amponya binti Yairo, na mama aliyeugua miaka 12. Marko 5.
238. Huwezi kutumikia mabwana wawili. Luka 16.
239. Mfano wa tajiri na Lazaro. Luka 16.
240. Kurudisha shukrani. Luka 17
241. Dhambi yaweza kumfuata mtu kanisani. Luka 18 na 21.
242. Zakayo mtu mfupi apanda mti. Luka 19
243. Imani ya mwanamke mkakanayo. Mathayo 15
244. Kulishwa kwa watu 4000 mikate na samaki mara ya pili. Marko 7-9
245. Kubeba msalaba na kukana nafsi. Marko 8, Mathayo 17
246. Wanafunzi washindwa kutoa pepo. Marko 9, Mathayo 17
247. Ni nani mkubwa katika ufalme wa Mungu. Marko 9
248. Je ni halali kumpa mke talaka au kuachana? Marko 10.

249. Waacheni watoto wadogo waje Kwangu. Mathayo 13, Marko 10
250. Kijana tajiri na mtawala. Marko 10. Mathayo 13.
251. Waajiriwa asubuhi na wale wa jioni, walipwa sawa sawa. Mathayo 20.
252. Kukaa mkono wa kuume au kushoto mbinguni. Mathayo 20, Marko 10.
253. Kipofu Batimayo. Mathayo 17. Luka 19
254. Kulipa kodi ni halali. Mathayo 22 na 24.
255. Twapasa kusamehe watu kama Mungu anavyotusamehe. Mathayo 18
256. Hosana mbarikiwa ajaye kwa Jina la BWANA. Mathayo 21
257. Mtini kukauka. Mathayo 21, Luka 20.
258. Mkulima mwenye shamba na watenda kazi waovu. Mathayo 21, Luka 20.
259. Masadukayo, ndoa na ufufuo . Luka 20.
260. Ipi ni amri kubwa kupita zingine. Mathayo 22.
261. Ole wa Mafarisayo. Mathayo 23.
262. Mafarisayo. Mathayo 23.
263. Yesu anarudi upesi, Je dalili za kuja Kwake ni zipi? Mathayo 24.
264. Dalili za siku za mwisho. Mathayo 24
265. Wanawali watano wajinga, na watano werevu. Mathayo 25
266. Kutumia talanta zetu ili ziwe na faida. Mathayo 25.
267. Hati ya kusafiria Mbinguni. Mathayo 25
268. Yesu anamfufua Lazaro I. Yohana 10 na 11
269. Wanapanga kumwua Yesu Yohana 11 na 12
270. Wayunani wanamtafuta Yesu. Yohana 11 na 12.
271. Kualikwa harusini. Mathayo 22. Luka 16.
272. Mwanakondoo aliyepotea, sarafu iliyopotea. Luka 14.
273. Mwana mpotevu au mtoto aliyekimbia kwao. Luka 15
274. BWANA aosha miguu. Mathayo 26 Yohana 13.
275. Pasaka ya mwisho. Yohana 13.
276. Msifadhaikeni mioyoni mwenu. Yohana 14
277. Yesu mzabibu wa kweli. Yohana 15, 16.
278. Sala ya Yesu kwetu wote. Yohana 17, Luka 22
279. Yesu anakamatwa. Luka 22
280. Yesu kwa Pilato. Luka 22.
281. Taji ya miiba. Yohana 19.
282. Yesu anakata roho. Yohana 19, Mathayo 27
283. Mazishi ya Yesu. Luka 23-24, Marko 15, Mathayo 27.
284. Kufufuka kwa YESU. Marko 16
285. Njia ya Emmaus. Luka 24
286. Simoni na Yohana wanaenda kaburi kuhakikisha. Yohana 21, Luka 24
287. Yesu awatokea wanafunzi Wake kwa siku 40. Mathayo 28, Matendo 1, Yohana 21.
288. Yesu amwimarisha Petro. Yohana 21.
289. Yesu Anapaa juu mbinguni. Mathayo 28, Luka 24, Marko 16 na Matendo 1.
290. Je Yesu anafanya nini mbinguni sasa? “Tuna Rafiki mbinguni.”
291. Kusimulia Kisa cha Wokovu kwa dakika tatu!
292. Kungoja Roho Mtakatifu/Pentekoste Yerusalemu. Luka 24, Matendo 1na 2.
293. Pentekoste. Matendo 1.

294. Petro anahubiri. Matendo 2.
295. Kiwete aruka ruka. Matendo 3
296. Mitume wanaingia Gerezani kwa mara ya kwanza. Matendo 4.
297. Anania na Safira. Matendo 5.
298. Mitume wawekwa gerezani mara mbili. Matendo 5.
299. Stefano auwawa. Matendo 6.
300. Sauli atesa watakatifu na kanisa. Matendo 8.
301. Filipo na towashi wa Ethiopia (Kushi). Matendo 8.
302. Sauli atokewa na Yesu. Matendo 9.
303. Tabitha au Dorkasi mama mkarimu afufuliwa. Matendo 10.
304. Kornelio wa mataifa Maombi yake yalisikiwa. Matendo 10.
305. Hakika Mungu hana upendeleo. Matendo 10.
306. Petro atolewa na malaika gerezani. Matendo 11-12.
307. Wayahudi wakataa injili, ukristo waenda kwa mataifa. Matendo 13-14.
308. Paulo apigwa mawe Lystra. Matendo 14
309. Baraza la Mitume laandika barua ihusuyo wamataifa wanaomwamini Yesu. Matendo 15.
310. Paulo na Sila waimba gerezani. Matendo 16.
311. Watu waliopindua ulimwengu juu chini. Matendo 17.
312. 312 Akila, Prisila, na Apolo. Matendo 18
313. Vitabu vya uovu vyachomwa moto. Matendo 19.
314. endo 19
315. Paulo awaaga waumini. Matendo 20
316. Paulo akamatwa. Matendo 21
317. Paulo ajitetea na kurudia Historia ya injili. Matendo 21, na 22
318. Masadukayo na Mafarisayo wamgombania Paulo. Matendo 22-23
319. Paulo aenda Kaisaria na Jeshi. Matendo 23
320. Paulo mbele ya Gavana Feliki. Matendo 24.
321. Paulo anakata rufani kwenda Rumi mbele ya Agripa. Matendo 24 na 25.
322. Paulo ashuhudia kisa chake tena. Matendo 26
323. Paulo amkatisha shauri Herode Agripa. Matendo 26 na 27.
324. Kuvunjikiwa merekebu na kuogelea. Matendo 27.
325. Kisiwani malta. Matendo 28
326. Paulo ashuhudia Rumi na kuandika barua kwa makanisa. Matendo 28.
327. Barua za Paulo, Mitume na Yuda na Yakobo.
328. Warumi. Tunaokolewa kwa Imani, kupitia Yesu tu! Si kwa matendo ya sheria.
329. Wakorintho wa kwanza. Shida za waumini wapya zajadiliwa.
330. Wakorintho wa pili. Tunapokuwa wanyonge ndiyo tuna nguvu.
331. Wagalatia. Tunda la Roho dhidi ya matendo ya mwili.
332. Waefeso. Mahusiano ya wazazi, watoto, wake, waume, mabwana na watumwa
333. Wafilipi. Furahini katika BWANA tena nasema furahini
334. Wakolosai. Kama tulivyompokea Kristo tuenende vivyo hivyo katika Yeye.
335. Wathesalonike. Tuombe bila kukoma
336. Wathesalonike wa pili. Asiyefanya kazi na asile.
337. Timotheo wa kwanza. Tabia ya Mchungaji na Shemasi.

338. Waraka Timotheo wa pili. Nimevipiga vita vizuri, Mwendo nimeumaliza, Taji inaningojea.
339. Waraka kwa Tito. Tabia ya mchungaji, tabia ya mzee wa kanisa..
340. Waraka kwa Filemoni. Msamehe Onesimo na mchukue kama Ndugu
341. Waraka kwa Waebrania. Yesu ni bora kupita vyote
342. Waraka wa Yakobo. Imani bila matendo ya kumpendeza Mungu, imekufa.
343. Waraka wa Petro wa kwanza
344. Waraka wa Petro wa pili.
345. Waraka wa Yohana wa kwanza. Tazameni pendo la ajabu! Mungu ni Upendo.
346. Waraka wa Yohana wa Pili
347. Waraka wa Yohana wa tatu. Naomba ufanikiwe katika mambo yote.
348. Waraka wa Yuda. MUNGU anaweza kutulinda tusijikwae, tukimruhusu.
349. UFUNUO. Upande wa Mungu unashinda, Mungu atahukumu na kuwazawadia watakatifu. Ufunuo 1-2.
350. Makanisa saba ya Asia Ndogo. Ufunuo 2-3
351. Ni nani awezaye kukifungua kitabu? Ufunuo 5, 8-10
352. Shetani alivyoanguka na malaika zake wakaja duniani. Ufunuo 12.
353. Mnyama wa kwanza na wa Pili. Ufunuo 13.
354. Malaika wanne na watakatifu 144,000. Ufunuo 14-17.
355. Kuepuka mafundisho ya uongo. Ufunuo 18-20.
356. Jehanamu I
357. Jehanamu II
358. Tazama maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu. Ufunuo 21.
359. Mbinguni milele na milele. Ufunuo 22.
360. Yerusalemu mpya yashuka chini, kila goti litapigwa kwa Mwenyezi MUNGU na Kila ulimi utakiri. Ufunuo 20-22. ya Yesu.
361. Yerusalemu mpya yashuka chini, kila goti litapigwa kwa Mwenyezi MUNGU na Kila ulimi utakiri.
362. Elimu ya Kikristo ndiyo ya Milele na bora kupita zote
363. Kufanya marafiki wa Mungu
364. Jinsi Mungu Anavyompenda Mwanadamu
365. Pambano Kuu Limekwisha, Kila kiumbe haina na kisicho hai wanakiri Mungu ni Upendo
366. Zoesha Ubongo wako Kufikiri mambo makubwa na ya Akili nyingi, Yale yahusuyo Muumba, utakuwa Jitu la akili nyingi! (Genius) na Hatua za Ufanisi katika Maisha Yako

**Watu 40 tofauti wameandika mawazo yanayofanana**

Biblia tunayotumia sasa ni nakala ya nakala. Hakuna vitabu vilivyopatika vilivyoandikwa awali na waandishi (original) toleo la King James Version ya mwaka 1611 lina mika 400 na lilirudiwa kuhaririwa miaka 240 iliyopitwa. Haijalishi toleo unalotumia, watu wengi hufurahia zaidi kuona jinsi unavyoliishi, kuliko ni toleo gani unalolisoma! Je! Unalitafsirije Neno la Mungu katika maisha yako. Je, wewe ni Mkristo kweli au unajifanya tu? Je utakuwa mtafsiri bora wa Maandiko?

Heshima , Uungwana, Adabu njema, TABIA NJEMA (ETIQUETTE)

**JINSI YA KUWA NA ADABU NJEMA**
**Mheshimu Mungu,**
**Heshimu watu,**
**Jiheshimu**
**Heshimu mali za watu**
**Uwe wakili mzuri wa Mali na viumbe vya MUNGU**
**Zinajumuisha yote yanayohusu tabia njema na kila mtu anakumbuka hayo juu!**
Huo ndiyo muhtasari wa adabu NJEMA.

**ADABU KWA WATOTO NA WATU WAZIMA AU UUNGWANA NDIYO NINI?**
Watoto na watu wakubwa,wanapaswa Kujua
Ukorofi wa mtoto wako sio wa kukusudia kila wakati.
Wakati mwingine watoto hawatambui ni kukosa adabu kukatiza, kuchokonoa pua zao, au kuzungumza kwa sauti ya juu wakiona kwamba mwanamke anayetembea mbele yao ana mguu mmoja!
Na kwa mahangaiko na misukosuko ya maisha ya kila siku, mama na baba walio na shughuli nyingi huwa hawana wakati wa kuzingatia ufundishaji wa adabu. Lakini ikiwa utaikazania Mambo haya 36 ya lazima, utalea mtoto mwenye adabu, mkarimu, anayependwa kwa neema ya MUNGU. Twajua uzazi ni mwenye dhambi mmoja kumkuza mwenye dhambi mwingine! Ila Neema ya MUNGU inatosha safarini!

1. Wakati wa kuuliza kitu, sema “Tafadhali au naomba.”
2. Unapopokea kitu, sema “Asante.”
3. Usisumbue watu wazima ambao wanazungumza isipokuwa kama una dharura. Wataijia shida yako na kukujibu watakapomaliza kuzungumza.
4. Ikiwa unahitaji kupata umakini wa mtu mara moja, “samahani” ndiyo njia ya adabu zaidi ya wewe kuingia kwenye mazungumzo yao.
5. Unapokuwa na shaka yoyote juu ya kufanya kitu, omba ruhusa kwanza. Inaweza kukuokoa kutoka kwa masaa mengi ya huzuni baadaye.
6. Ulimwengu hauna nia ya kile usichokipenda. Weka maoni hasi kwako, au kati yako na marafiki zako, na nje ya masikio ya watu wazima.usipende ulalamishi
7. Usitoe maoni juu ya tabia za watu wengine isipokuwa, kuwapongeza, ambayo inakubalika kila wakati ikiwa una hasi mchukue pembeni kwa maneno ya upendo mwambie.
8. Wakati watu wanakuuliza hali yako, waambie, usikae kimya ukisalimiwa, kisha uwaulize hali zao.
9. Unapotumia wakati nyumbani mwa rafiki yako, kumbuka kuwashukuru wazazi wake kwa kuwa wamekupenda kukupa wakati mzuri uliokuwa nao.
10. Bisha kwenye milango iliyofungwa - na subiri kuona ikiwa kuna majibu - kabla ya kuingia. Na hasa chooni.
11. Unapopiga simu, jitambulishe kwanza kisha uulize ikiwa unaweza kuzungumza na mtu unayempigia.

12. Kuwa na shukrani na sema "asante" kwa zawadi yoyote unayopokea. Waweza kutumia barua-pepe,au barua ya shukrani iliyoandikwa kwa mkono inaweza kuwa nan mvuto mkubwa.
13. Kamwe usitumie lugha chafu mbele ya watu wazima. Watu wazima tayari wanajua msamiati huo wote, matusi sio maneno halisi au kweli bali ni vimaneno vya kutaka kumkasirisha mtu na basi vimaneno vyenyewe havifurahishi.
14. Usiite watu majina ya kashifa. Wakolosai 4: 5-6
15. Usimdhihaki mtu yeyote kwa sababu yoyote. Kumdhihaki kunaonyesha wengine kuwe wewe u dhaifu, na kumwandikia mtu mwingine ni ukatili. Waefeso 4:29
16. Hata kama mchezo au mkusanyiko ni wa kuchosha, kaa kwa utulivu na ujifanye unavutiwa. Wasanii na watangazaji wanafanya bidii na wanachukua mida yao, labda yale wayafanyayo yanapingana na imani yako.
17, Ukipigana vikumbo na mtu, sema mara moja "Samahani."
18. Funika mdomo wako wakati wa kukohoa au kupiga chafya, na usichokonoe pua yako hadharani.Pia usikojoe hadharani labda kuwe na dharura tu!
19. Unapopita mlangoni, angalia ikiwa unaweza kumfungulia mtu mwingine mlango.
20. Ukikutana na mzazi, mwalimu, au jirani akifanya kazi au jambo fulani, uliza ikiwa unaweza kusaidia. Ikiwa wanasema "ndio," fanya hivyo - unaweza kujifunza kitu kipya. Na wakati mwingine angalia hali na anza kusaidia, labda ukatazwe.
21. Wakati mtu mzima anakuuliza msaada, fanya bila kunung'unika na kwa tabasamu.
22. Mtu anapokusaidia, sema "asante." Mtu huyo atataka kukusaidia tena. Hii ni kweli haswa kwa waalimu shuleni, kanisani na jamii. Waandikie shukurani ya dhati wakati mwingine
23. Tumia vyombo vya kula vizuri. Ikiwa haujui jinsi ya kufanya hivyo, waombe wazazi wako wakufundishe au waangalie kile watu wazima hufanya-kisu, uma, kijiko.
24. Weka kitambaa kwenye mapaja yako; na kitumie kuifuta midomo wako inapobidi (huu ni utamaduni wa wenye hivi vitu).
25. Usichukue vitu mezani vilivyo mbali; uliza chakula kipitishwe.
Salamia watu, sasa kwa sababu ya kushikana mkono kwa Corona imeondolewa, lakini usipuuze watu wanapokujulia hali au wanapotaka mawasiliano
27. Usiwe mtu wa jazba au ugomvi, na ukitokea ugomvi tafuta njia ya kusuluhisha na kuwa mtengeneza amani. Wakolosai 1: 20-21
Kuwa mwema, na mwenye adabu kwa masikini, wahitaji, wageni, wajane na yatima
Kuwa na heshima kwa wote, na ujue jinsi ya kuzungumza na wale ambao ni wakubwa kwako. 2 Wafalme 2: 23-24. Mambo ya Walawi 19:32
30. Usiwe mvivu, kila wakati uwe mchapakazi, usile jasho la wengine 2 Wathesalonike 3: 7-10
31. Heshimu watu wake/waume wa wengine kwa maneno na matendo. Epuka kuwa na tabia mbovu za uchafu wa moyo.
32. Heshimu maisha ya wengine na viumbe, usiwadhuru kwa njia yoyote. Labda wawe panya, mbu au mende yaani wanyama wa kudhuru. 1 Wakorintho 13: 5
33. Heshimu mali ya watu wengine unapowatembelea, Wafilipi 2: 3

34. Heshimu sheria za nyumba unayotembelea, na uombe ruhusa ikiwa lazima uende na watoto wao au uwape chakula au zawadi
35. Watendee wengine vile ungetaka wakutendee wewe. 1 Petro 3: 8
36. Watendee watu ambao hawastahili fadhili kwa wema nao wataona aibu na kujifunza Luka 6:32

## VITAFUNIO MBALIMBALI

Muhimu kuzingatiwa katika huduma ya Muziki
1. Muziki wa waumini ni muhimu uonyeshe heshima na kicho kwenye ibada kwani ndio wakati tunakutana na Mungu, Na pia uendane na Maandiko matakatifu, na si kutunga vitu vinavyokiuka Maandiko.
2. Vyombo vya Muziki vichezwe kwa upatanifu na visisikike juu zaidi na kuzuia maneno ambayo ndiyo yamebeba ujumbe wa Mungu.
3. Muziki unapotolewa uonyeshe Furaha na uchangamfu wa kuwa mbele za Mungu (Uf. 7:12)
4. Uwiano uwepo katika Ujumbe unaotolewa na mpangano wa Sauti na ulete somo mahususi linaloweza kueleweka
5. Waimbaji wa Kwaya ya Kanisa na Vikundi wawe na sare kadri iwezekanavyo au mavazi ya heshima ya kujiwasilisha vizuri mbele ya watu na Mbele za Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana.
6. Muziki na huduma ya Uimbaji katika maandiko ni sawa kama Sadaka ya Shukrani kwa Mungu kwa Uumbaji, ulinzi Wake Mungu na Wokovu wa Milele. Angalia kwaya ya watu 4000 ilikuwa inafanya kazi kama Watumishi wa BWANA.
7. Hebu tufanye matengenezo ya kuturejesha katika mapito ya zamani wa Muziki wa Kiadiventista. (Yeremia 6:16.) Mungu na awabariki.

MUNGU AWE NASI.

**Kanuni za familia yetu**
**Sally Clarkson**

**Kuhusu mamlaka ya nyumba yetu**
Tunampenda na kumtii Mungu, kwa mioyo yetu yote
Tunasoma Neno la Mungu na kuomba kila siku na moyo mkunjufu
Tunawaheshimu na kuwatii wazazi wetu na ari njema
Tunasikiliza mausia na kukubali adhabu kwa roho ya unyenyekevu

**Kuhusu mahusiano kwenye familia yetu**
Tunapendana na kuchukuliana kwa wema, upole na adabu
Tunahudumiana kwa unyenyekevu, tukifikiria mahitaji ya mwenzetu kwanza
Tunatiana moyo, kwa kutumia maneno ya kujenga na kubariki.
Tunasameheana, na kuyasahau hayo kwa upendo hata pale tulipoumizwa na kukwazwa

**Kuhusu umilikaji wa familia yetu**
Tunamshukuru Mungu kwa vyote tulivyonavyo, vidogo au vikubwa

Tunaridhika na tulivyonavyo, hatutamani walivyonavyo wengine
11.Tu wakarimu kwa tulivyanavyo, tunashirikiana na wengine kwa moyo mkunjufu.Tunasaidiana kwa tulivyo navyo, tukivitumia kwa hekima na kuwajibika

**Kuhusu Kazi katika familia yetu**
Tunanuia kumaliza kazi tuliyopewa kwa uaminifu na kwa muda wake.
Tunanuia kumaliza kazi tuliyopewa, bila ya kukumbushwa-kumbushwa
Tunafanya kazi kwa moyo mkunjufu, tunasaidiwa na kusaidia wengine bila kinyongo
Tunachukua jukumu la kuweka nyumba yetu nadhifu na safi wakati wote

**Kuhusu mtazamo wa familia yetu**
Tunachagua kuwa wacheshi, hata pale tunapojaribiwa kunung'unika
Tunachagua kuwa wapatanishi, hata tupatapo majaribu ya kubishana-bishana
Tunachagua kuwa wavumilivu, kinyume cha nia zetu
Tunachagua kuwa watu wa shukrani, kinyume cha vishawishi vya kibinadamu

**Kuhusu uchaguzi wa familia yetu**
Tunafanya yale ambayo yanapasa haki, hata wengine wakitushawishi mengine
Tunauliza kabla ya kutenda, pale ambapo hatujui lile jema kulifanya
Tunatawala nafsi kwa hali na mali wakati wote
Tunasema kweli daima, na kuepuka ulaghai wa aina yoyote
Tukienda popote kwa wengine, tunafanya haya 21 mema kama vile tupo kwetu
Tukikiuka au kusahau sheria 21 za Nyumba hii, tunakubali hatua za nidhamu na maagizo toka kwa Mungu.

**Ahadi za Biblia tunazopaswa  Kuzidai kwenye Maombi**

***Ahadi za Roho Mtakatifu***
"Mwombeni Bwana mvua wakati wa masika, naam, Bwana afanyaye umeme, Naye atawapa manyunyu ya mvua, kila mtu atapewa nyasi kondeni." Zakaria 10:1

"Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" Luka 11:13

"Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa Jina Langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia… Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu." Yohana 14:26; 16:8

"Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lolote kwa Jina Langu, nitalifanya." Yohana 14:12 – 14

"Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo Neno la Bwana kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho Yangu, asema Bwana wa

majeshi." Zakaria 4:6

Ahadi kwamba Mungu Hujibu Maombi "Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa." Yohana 15:7

"Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji." Waebrania 4:16

"Kwa sababu hiyo nawaambia, Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24

"Ukaniite siku ya mateso; Nitakuokoa, na wewe utanitukuza." Zaburi 50:15 "Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba Yangu aliye mbinguni." Mathayo 18:19

"Na yoyote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea." Mathayo 21:22 "

Nanyi mkiomba lo lote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa Jina Langu, nitalifanya." Yohana 14:13, 14 20 "

Tena siku ile hamtaniuliza neno lo lote. Amin, amin, nawaambia, Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa Jina Langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa Jina Langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu." Yohana 16:23, 24

"Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba." 1 Yohana 5:14, 15

***Ahadi kuhusu Nguvu ya Mungu***

"Kuna Neno gani lililo gumu la kumshinda Bwana? Kwa muhula wake nitakurudia, wakati huu huu mwakani, na Sara atapata mwana wa kiume." Mwanzo 18:14

"Bwana atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya." Kutoka 14:14

"Yesu akawakazia macho, akasema, Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyo; maana yote yawezekana kwa Mungu." Marko 10:27

"Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya." 1 Wathesalonike 5:24
"Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika." Ayubu 42:2

"Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? Yeye asiyemwachilia Mwana Wake Mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja Naye?" Warumi 8:31, 32

"Mungu si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena, hatalifikiliza?" Hesabu 23:19

"Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki; akili zake hazichunguziki. Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo. Hata vijana watazimia na kuchoka, na wanaume vijana wataanguka; bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia." Isaya 40:28 – 31

***Ahadi za Uongozi wa Mungu***

"Je! Si Mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, Yu pamoja nawe kila uendako." Yoshua 1:9

"Na tazama, Mimi Nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, Nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia." Mwanzo 28:15 21

"Tazama, Mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengezea." Kutoka 23:20

"Lakini huko, kama mkimtafuta Bwana, Mungu wako, utampata, ukimtafuta kwa moyo wako wote, na roho yako yote." Torati 4:29
"Niite, Mami nitakuitikia, Mami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua." Yeremia 33:3

"Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza patasawazishwa; Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja; Kwa kuwa kinywa cha Bwana kimenena haya." Isaya 40:4, 5

"Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; Nitakushauri, jicho Langu likikutazama." Zaburi 32:8 "Naye Bwana, Yeye Ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaike." Torati 31:8

"Ni nani amchaye Bwana? Atamfundisha katika njia anayoichagua." Zaburi 25:12

"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri Yeye, Naye atayanyosha mapito yako." Mithali 3:5, 6

"Na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui." Isaya 58:10, 11

"Nao watatoka nje na kuitazama mizoga ya watu walioniasi; maana funza wao hatakufa, wala moto wao hautazimika nao watakuwa chukizo machoni pa wote wenye mwili." Isaya 65:24

***Ahadi za Moyo Uliobadilishwa***

"Nami nitawapa moyo, wanijue ya kuwa Mimi ni Bwana; nao watakuwa watu Wangu, Nami nitakuwa Mungu wao; kwa maana watanirudia kwa moyo wao wote." Yeremia 24:7

"Bwana, Mungu wako, atautahiri moyo wako, na moyo wa uzao wako, ili umpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, upate kuwa hai." Torati 30:6 22

"Nami nitawapa ninyi moyo mpya, Nami nitatia roho mpya ndani yenu, Nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, Nami nitawapa moyo wa nyama." Ezekieli 36:26 "

Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu;" Wafilipi 1:6

"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya." 1 Wakorintho 5:17

"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi Yake kwa ajili yangu." Wagalatia 2:20

"Mungu wa amani Mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja Kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni Mwaminifu ambaye awaita, Naye atafanya." 1 Wathesalonike 5:23, 24

***Ahadi za Msamaha***
"Ikiwa watu Wangu, walioitwa kwa Jina Langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao." 1 Nyakati 7:14

"Kwa maana Wewe, Bwana, U mwema, Umekuwa tayari kusamehe, Na mwingi wa fadhili, Kwa watu wote wakuitao." Zaburi 86:5

"Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu." Marko 11:25

"Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi." Waefeso 4:32

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni Mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yohana 1:9

"Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu." Isaya 1:18

"Mimi, naam, Mimi, Ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili Yangu Mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako." Isaya 43:25 "Maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena." Yeremia 31:34 23 "Katika Yeye huyo, kwa damu Yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake." Waefeso 1:7

***Ahadi za Ushidi Dhidi ya Dhambi***
"Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu." 1 Yohana 5:4

"Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda." Warumi 8:37

"Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo." 1 Wakorintho 15:57 "

Usiogope, kwa maana Mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana Mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki Yangu." Isaya 41:10

"Zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu." Waefeso 6:16

"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi Yake kwa ajili yangu." Wagalatia 2:20

"Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda

kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema." Wafilipi 2:13

"Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili." Wagalatia 5:16

"Naye Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi. Amina." Warumi 16:20

"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu." Warumi 12:2

"Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake." 1 Yohana 2:15

Ahadi za Uponyaji "Akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zZke, na kutega masikio usikie maagizo Yake, na kuzishika amri Zake, Mimi sitatia juu yako maradhi yo yote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi Ndimi Bwana nikuponyaye." Kutoka 15:20 "

Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba; Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako." Torati 33:25

"Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, Wala usizisahau fadhili Zake zote. Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote, Aukomboa uhai wako na kaburi, Akutia taji ya fadhili na rehema, Aushibisha mema uzee wako, Ujana wako ukarejezwa kama tai." Zaburi 103:2 – 5

"Usiwe mwenye hekima machoni pako; Mche Bwana, ukajiepushe na uovu. Itakuwa afya mwilini pako, Na mafuta mifupani mwako." Mithali 3:7, 8

"Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama Mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Isaya 53:3-5

"Uniponye, Ee Bwana, nami nitaponyeka; uniokoe, nami nitaokoka; kwa maana Wewe Ndiwe uliye sifa zangu." Yeremia 17:14

"Maana nitakurudishia afya, Nami nitakuponya jeraha zako, asema Bwana, kwa sababu wamekuita, mwenye kutupwa, wakisema, Ni Sayuni, ambao hapana mtu autakaye." Yeremia 30:17

"Tazama, nitauletea afya na kupona, Nami nitawaponya; nami nitawafunulia wingi wa amani na Kweli." Yeremia 33:6

"Lakini kwenu ninyi mnaolicha Jina Langu, jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa Zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa

mazizini." Malaki 4:2

"Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa Jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa." Yakobo 5:14, 15

***Ahadi kwa ajili ya Nguvu za Kufanya Mapenzi ya Mungu***
"Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele." 2 Wakorintho 4:16-18

"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho." Wagalatia 6:9

"Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu." Wafilipi 4:13

"Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema." Wafilipi 2:13

"Naye akaniambia, Neema Yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu." 2 Wakorintho 12:9

***Ahadi Kuhusu Kuwa Mashahidi wa Mungu***
"Msiogope wala msifanye hofu; je! Sikukuhubiri haya zamani na kuyaonyesha? Na ninyi ni mashahidi Wangu. Je! Yuko
Mungu zaidi Yangu Mimi? Hakika hapana Mwamba; Mimi sijui mwingine." Isaya 44:8

"Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia." Isaya 60:1

"Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi Yake kwa Kristo, Naye alitupa huduma ya upatanisho." 2 Wakorintho 5:18

"Lakini Bwana akaniambia, Usiseme, Mimi ni mtoto; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila Neno nitakalokuamuru." Yeremia 1:7

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." Matendo 1:8

"Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu." 1 Petro 2:9

"Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu." 1 Petro 3:15

**<u>Mafundisho Makuu ya BIBLIA</u>**

**Kanisa linaikubali Biblia kama tamko lake la pekee la imani na inayashikilia Mafundisho Makuu ya Imani kuwa ndiyo Mafundisho ya Maandiko Matakatifu. Imani hizi kama zilivyoelezwa hapa, zinajumuisha uelewa wa kanisa na namna linavyoyaeleza mafundisho ya Maandiko. Mapitio ya Matamko haya yanaweza kutarajiwa kwenye kikao cha viongozi wa Kanisa la kiulimwengu wakati kanisa linapoelekezwa na Roho Mtakatifu kwenye uelewa ulio mkamilifu wa Kweli ya Biblia au inapopata lugha iliyo bora zaidi ya kuelezea mafundisho ya Neno Takatifu la Mungu.**

**<u>1. Maandiko Matakatifu:</u>**
**Maandiko Matakatifu, yaani Agano la Kale na Jipya, ndiyo Neno la Mungu lililoandikwa na kisha likatolewa kwa uvuvio wa Mungu, kupitia kwa watu watakatifu wa Mungu walionena na kuandika kama walivyoongozwa na Roho Mtakatifu. Ndani ya Neno hili Mungu amemkabidhi mwanadamu maarifa yaliyo ya lazima kwa ajili ya wokovu. Maandiko Matakatifu ni ufunuo thabiti wenye mamlaka wa mafundisho ya imani na kumbukumbu aminifu ya matendo ya Mungu katika historia.**
**(2 Petro 1:20, 21; 2 Tim. 3:16, 17; Zab. 119:105; Mith. 30:5, 6; Isa. 8:20; Yoh. 17:17; 1 Thess. 2:13; Waebr. 4:12.)**

**<u>2. Utatu Mtakatifu:</u>**
**Kuna Mungu mmoja: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, umoja wa Nafsi tatu za milele. Mungu hapatikani na mauti, mwenye nguvu zote, ajuaye yote, aliye juu ya yote, na aliyeko daima. Yeye hana mwisho na ni zaidi ya ufahamu wa kibinadamu, hata hivyo anafahamika kupitia kujifunua Kwake Binafsi. Milele zote yu astahili kuabudiwa, kusujudiwa, na kutumikiwa na viumbe wote.**
**(Kumb. 6:4; Math. 28:19; 2 Kor. 13:14; Efe. 4:4-6; 1 Petro 1:2; 1 Tim. 1:17; Ufu. 14:7.)**

**<u>3. Baba:</u>**
**Mungu Baba wa milele Ndiye Muumbaji, Chimbuko, Mtegemezaji na Mfalme wa viumbe vyote. Ni mwenye haki na mtakatifu, mwingi wa rehema, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, na mwingi wa uthabiti wa upendo na uaminifu. Tabia na uwezo vilivyodhihirishwa ndani ya Mwana na ndani ya Roho Mtakatifu pia ni ufunuo wa Baba.**

**(Mwa. 1:1; Ufu. 4:11; 1 Kor. 15:28; Yoh. 3:16; 1 Yoh. 4:8; 1 Tim. 1:17; Kut. 34:6, 7; Yoh. 14:9.)**

**4. Mwana:**

**Mungu Mwana wa milele alifanyika mwili katika Yesu Kristo. Kupitia Kwake vitu vyote viliumbwa, tabia ya Mungu imefunuliwa, wokovu wa mwanadamu unakamilishwa na ulimwengu unahukumiwa. Milele zote Mungu kweli, alifanyika Mwanadamu kweli, Yesu aliye Kristo. Alichukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na kuzaliwa na bikira Mariamu. Akaishi na kupitia uzoefu wa majaribu kama mwanadamu, lakini kwa ukamilifu alionyesha kwa mfano haki na upendo wa Mungu. Kwa miujiza Yake alidhihirisha uwezo wa Mungu na alithibitishwa kama Masihi aliyeahidiwa. Aliteseka na kufa kwa hiari msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, na kama mbadala wetu, alifufuliwa kutoka katika wafu, na akapaa kuhudumu katika hekalu la mbinguni kwa niaba yetu. Atakuja tena katika utukufu kwa ajili ya ukombozi wa mwisho wa watu wake na urejeshwaji wa vitu vyote.**
**(Yoh. 1:1-3, 14; Kol. 1:15-19; Yoh. 10:30; 14:9; War. 6:23; 2 Kor. 5:17-19; Yoh. 5:22; Luka 1:35; Fil. 2:5-11; Waeb. 2:9-18; 1 Kor. 15:3, 4; Waeb. 8:1, 2; Yoh. 14:1-3.)**

**5. Roho Mtakatifu:**
**Mungu Roho wa Milele alikuwa mtendaji pamoja na Baba na Mwana katika Uumbaji, kufanyika mwili, na katika ukombozi. Aliwavuvia waandishi wa Maandiko Matakatifu. Aliyajaza maisha ya Kristo na uwezo. Huwavuta na kuwasadikisha wanadamu; na wale wanaoitikia huwafanya upya na kuwabadilisha wawe na sura ya Mungu. Akitumwa na Baba na Mwana ili kuwa siku zote na watoto Wake, hutoa karama za kiroho kwa kanisa, huliwezesha kumshuhudia Kristo, na kwa kupatana na Maandiko huliongoza kwenye Ukweli wote.**

**(Mwa. 1:1, 2; Luka 1:35; 4:18; Mat. 10:38; 2 Petro 1:21; 2 Kor. 3:18; Efes. 4:11, 12; Mat. 1:8; Yoh. 14:16-18, 26; 15:26, 27; 16:7-13.)**

**6. Uumbaji:**
**Mungu ni Muumba wa vitu vyote, na amefunua katika Maandiko uhalisi wa tukio la shughuli Zake za uumbaji. Katika siku sita Bwana alizifanya "mbingu na nchi" na vitu vyote vilivyo hai juu ya nchi, akastarehe siku ya saba ya juma lile la kwanza. Na hivyo akaanzisha Sabato kama kumbukumbu ya milele ya kukamilika kwa kazi Yake ya uumbaji. Mwanaume na mwanamke wa kwanza walifanywa kwa mfano wa Mungu kama upeo wa kazi Yake ya uumbaji, wakapewa utawala juu ya ulimwengu, na wakaagizwa kuwajibika na utunzaji Wake. Wakati ulimwengu ulipomalizika kila kitu kilikuwa ni "chema sana," kikitangaza utukufu wa Mungu.**

**(Mwa. 1; 2; Kut. 20:8-11; Zab. 19:1-6; 33:6, 9; 104; Waeb. 11:3.)**

**<u>7. Asili ya Mwanadamu:</u>**

**Mwanaume na mwanamke waliumbwa kwa mfano wa Mungu kila mmoja akiwa na nafsi yake, uwezo wake, na uhuru wake wa kufikiri na kutenda. Ingawa waliumbwa viumbe huru, kila mmoja ni muunganiko usiogawanyika wa mwili, akili, na roho, akimtegemea Mungu kwa uhai na pumzi na mengine yote. Wakati wazazi wetu wa kwanza walipomwasi Mungu, walikana utegemezi wao kwa Mungu na wakaanguka kutoka hadhi yao ya juu iliyokuwa chini tu ya Mungu. Sura ya Mungu iliyokuwa ndani yao ikaharibiwa na wakawa chini ya mauti. Wazao wao hushiriki asili hii ya anguko na matokeo yake. Wanazaliwa wakiwa na udhaifu na mivuto ya kuelekea kwenye uovu. Lakini Mungu katika Kristo aliupatanisha ulimwengu na nafsi yake, na kwa njia ya Roho Wake hurejesha ndani ya wanadamu watubuo sura ya Muumba wao. Wakiwa wameumbwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu, wanaitwa kumpenda na kupendana wao kwa wao, na kutunza mazingira yao.**

**(Mwa. 1:26-28; 2:7; Zab. 8:4-8; Mat. 17:24-28; Mwa. 3; Zab. 51:5; War. 5:12-17; 2 Kor. 5:19, 20; Zab. 51:10; 1 Yoh. 4:7, 8, 11, 20; Mwa. 2:15.)**

**<u>8. Pambano Kuu:</u>**

**Jamii yote ya wanadamu sasa inahusika katika pambano kuu baina ya Kristo na Shetani lihusulo tabia ya Mungu, sheria Yake, na ukuu Wake juu ya ulimwengu. Pambano hili lilianzia mbinguni wakati kiumbe aliyeumbwa na kutunukiwa uhuru wa kuchagua, katika kujiinua akawa Shetani, mpinzani wa Mungu, na kuwaongoza kwenye uasi sehemu ya malaika. Alianzisha roho ya uasi katika ulimwengu huu pale alipowaongoza Adamu na Hawa kuingia dhambini. Dhambi hii ya mwanadamu ilisababisha uharibifu wa sura ya Mungu katika wanadamu, uvurugaji wa mpangilio wa ulimwengu ulioumbwa, na mwishowe kuteketea wakati wa gharika iliyoikumba dunia hii. Ukitazamwa na ulimwengu wote ulioumbwa, ulimwengu huu ukawa uwanja wa vita wa malimwegu yote, ambao kutokana na vita hiyo Mungu wa upendo hatimaye atathibitika kuwa mwenye haki. Ili kuwasaidia watu Wake katika pambano hili, Kristo anamtuma Roho Mtakatifu na malaika watiifu kuwaongoza, kuwalinda, na kuwategemeza katika njia ya wokovu.**
**(Ufu. 12:4-9; Isa. 14:12-14; Eze. 28:12-18; Mwa. 3; War. 1:19-32; 5:12-21; 8:19-22; Mwa. 6-8; 2 Petro 3:6; 1 Kor. 4:9; Waeb. 1:14.)**

**<u>9. Maisha, Kifo, na Ufufuo wa Kristo:</u>**

**Katika maisha ya Kristo ya utii mkamilifu kwa mapenzi ya Mungu, mateso yake, mauti, na ufufuo, Mungu alitoa njia pekee ya kafara kwa ajili ya dhambi ya mwanadamu, ili wale ambao kwa imani wanapokea upatanisho huu waweze kuwa na uzima wa milele, na ulimwengu wote uweze kuelewa**

**vizuri zaidi upendo mtakatifu na usio na ukomo wa Muumbaji. Kafara hii kamilifu huthibitisha haki ya sheria ya Mungu na fadhili za tabia Yake; kwa kuwa hufanya yote mawili; kuhukumu dhambi yetu na kutupatia msamaha. Kifo cha Kristo ni cha mbadala na cha kulipia, cha kupatanisha na cha kubadilisha. Ufufuo wa Kristo hutangaza ushindi wa Mungu dhidi ya nguvu za uovu, na kwa wale wanaopokea kafara hujihakikishia ushindi wao wa mwisho dhidi ya dhambi na mauti. Hutangaza Ubwana wa Yesu Kristo, ambaye mbele Yake kila goti la mbinguni na duniani litapigwa. (Yoh. 3:16; Isa. 53; 1 Petro 2:21, 22; 1 Kor. 15:3, 4, 20-22; 2 Kor. 5:14, 15, 19-21; War. 1:4; 3:25; 4:25; 8:3, 4; 1 Yoh. 2:2; 4:10; Kol. 2:15; Waf. 2:6-11.)**

**<u>10. Uzoefu wa Wokovu:</u>**
**Katika upendo usio na ukomo na rehema Zake Mungu alimfanya Kristo, asiyejua dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili kwamba katika yeye tuweze kufanywa haki ya Mungu. Tukiongozwa na Roho Mtakatifu tunatambua hitaji letu, tunakiri hali yetu ya kuwa wenye dhambi, tunatubu maasi yetu, na kuonesha imani katika Yesu kama Bwana na Kristo, kama Mbadala na Kielelezo. Imani hii inayopokea wokovu huja kupitia katika uwezo wa kimbingu wa Neno na ni karama ya neema ya Mungu. Kupitia kwa Kristo tunahesabiwa haki, tunafanywa kuwa wana na binti za Mungu, na kukombolewa kutoka katika hali ya kuwa chini ya dhambi. Kupitia kwa Roho tunazaliwa upya na kutakaswa; Roho hufanya upya nia zetu, huandika sheria ya Mungu ya upendo katika mioyo yetu, na tunapewa uwezo wa kuishi maisha matakatifu. Tukikaa ndani Yake, tunakuwa washirika wa asili ya Uungu na tuna hakika ya wokovu sasa na katika hukumu.**
**(2 Kor. 5:17-21; Yoh. 3:16; Wag. 1:4; 4:4-7; Tito 3:3-7; Yoh. 16:8; Wag. 3:13, 14; 1 Petro 2:21, 22; War. 10:17; Luk. 17:5; Mark 9:23, 24; Waef. 2:5-10; War. 3:21-26; Kol. 1:13, 14; War. 8:14-17; Wag. 3:26; Yoh 3:3-8; 1 Petro 1:23; War. 12:2; Waeb. 8:7-12; Eze. 36:25-27; 2 Petro 1:3, 4; War. 8:1-4; 5:6-10.)**

**<u>11. Kukua katika Kristo:</u>**
**Kwa kifo chake msalabani Yesu alizishinda nguvu za uovu. Yeye aliyewatiisha pepo wachafu wakati wa huduma Yake hapa duniani, amezivunja nguvu zao na kuthibitisha kuwa mwisho wao ni uangamivu usioepukika. Ushindi wa Yesu hutupatia ushindi dhidi ya nguvu za uovu ambazo bado zinatafuta kututawala, tunapotembea Naye kwa amani, furaha, na uhakika wa upendo wake. Sasa Roho Mtakatifu anakaa ndani yetu na kututia nguvu. Tukidumu kujikabidhi kwa Yesu kama Bwana na Mwokozi wetu tunawekwa huru kutoka katika mzigo wa matendo yetu yaliyopita. Hatuishi tena gizani, katika hofu ya nguvu za uovu ujinga na katika kukosa maana kwa namna ya maisha yetu ya awali. Katika uhuru huu mpya ndani ya Kristo, tumeitwa kukua katika kufanana na tabia Yake, tukiongea Naye kila siku katika sala, na kujilisha Neno lake, tukilitafakari Neno Lake na majaliwa Yake, tukiimba sifa Zake, tukikusanyika pamoja kwa ajili ya ibada, na kushiriki katika utume wa kanisa. Tukijitoa katika**

**kuwahudumia kwa upendo wale wanaotuzunguka na katika kuwashuhudia wokovu Wake; kuwepo Kwake nasi daima kwa njia ya Roho hugeuza kila wasaa na kila kazi kuwa uzoefu wa kiroho.**
**(Zab. 1:1, 2; 23:4; 77:11, 12; Kol 1:13, 14; 2:6, 14, 15; Luk. 10:17-20; Waef. 5:19, 20; 6:12-18; 1 Wath. 5:23; 2 Petro 2:9; 3:18; 2 Wak. 3:17, 18; Waf. 3:7-14; 1 Wath. 5:16-18; Math. 20:25-28; Yoh. 20:21; Wag. 5:22-25; War. 8:38, 39; 1 Yoh. 4:4; Waeb. 10:25.)**

**12. Kanisa:**
**Kanisa ni jamii ya waumini wanaomkiri Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi. Katika mwendelezo wa kufungamana na watu wa Mungu wa nyakati za Agano la Kale, tunaitwa kutoka duniani; na tunajiunga pamoja kwa ajili ya ibada, kwa ajili ya ushirika, kwa ajili ya mafundisho katika Neno, na kwa ajili ya adhimisho la Meza ya Bwana, kwa ajili ya huduma kwa wanadamu wote, na kwa ajili ya mbiu ya injili kwa ulimwengu wote. Kanisa linapata mamlaka yake kutoka kwa Kristo, ambaye ni Neno lililofanyika mwili, na kutoka katika Maandiko, ambayo ndiyo Neno lililoandikwa. Kanisa ni familia ya Mungu; iliyofanywa Naye kuwa watoto Wake, huku washiriki Wake wakiishi katika msingi wa Agano Jipya. Kanisa ni mwili wa Kristo, jamii ya wenye imani ambayo Kristo Mwenyewe Ndiye kichwa. Kanisa ni bibi arusi ambaye Kristo alimfia ili apate kumtakasa na kumsafisha. Wakati wa kurudi Kwake kwa ushindi, ataliwasilisha Kwake Mwenyewe kanisa lenye utukufu, waaminifu wa karne zote, walionunuliwa kwa damu Yake, likiwa halina waa wala kunyanzi, bali likiwa takatifu na lisilo na ila.**
**(Mwa. 12:3; Mat. 7:38; Waef. 4:11-15; 3:8-11; Math. 28:19, 20; 16:13-20; 18:18; Waef. 2:19-22; 1:22, 23; 5:23-27; Wakol. 1:17, 18.)**

**13. Masalio na Utume Wake:**
**Kanisa la kiulimwengu linajumuisha wale wote ambao wanamwamini Kristo kiukweli, ila katika siku za mwisho, kipindi cha kuenea kwa ukengeufu, masalio wameitwa kuzishika Amri za Mungu na Imani ya Yesu. Masalio hawa hutangaza kuwadia kwa saa ya hukumu, hutangaza wokovu kupitia Kristo, na hupiga mbiu ya kukaribia kwa marejeo Yake ya pili. Tangazo hili huwakilishwa na mfano wa malaika watatu wa Ufunuo 14; nayo huambatana na kazi ya hukumu mbinguni isababishayo kazi ya toba na matengenezo duniani. Kila muumini ameitwa kuwa na sehemu binafsi katika ushuhuda huu uendao ulimwenguni kote.**
**(Ufu. 12:17; 14:6-12; 18:1-4; 2 Kor. 5:10; Yuda 3, 14; 1 Petro 1:16-19; 2 Petro 3:10-14; Ufu. 21:1-14.)**

**14. Umoja katika mwili wa Kristo:**
**Kanisa ni mwili mmoja ulio na washiriki wengi, walioitwa kutoka kila taifa, kabila, lugha, na jamaa. Katika Kristo tu viumbe vipya; kubaguana kwa rangi, tamaduni, elimu, na utaifa, na tofauti baina ya tabaka la juu na la**

**chini, tajiri na maskini, mwanamme na mwanamke, havipaswi kutuletea mgawanyiko katikati yetu. Sote tu sawa katika Kristo, ambaye kwa Roho mmoja ametufunga katika ushirika mmoja pamoja Naye na sisi wenyewe kwa wenyewe; tunapaswa kutumika na kutumikiwa pasipo upendeleo au kusitasita. Kupitia kwa ufunuo wa Yesu Kristo katika maandiko tunashiriki imani na tumaini moja, na tunawafikia wote kwa ushuhuda mmoja. Umoja huu una chimbuko lake katika umoja wa Mungu Mmoja Mwenye nafsi tatu ambaye ametufanya sisi kuwa watoto Wake.**
**(War. 12:4, 5; 1 Kor. 12:12-14; Math. 28:19, 20; Zab. 133:1; 2 Kor. 5:16, 17; Mat. 17:26, 27; Wag. 3:27, 29; Kol. 3:10-15; Waef. 4:14-16; 4:1-6; Yoh. 17:20-23.)**

**15. Ubatizo:**

**Kwa njia ya ubatizo tunakiri imani yetu katika kifo na ufufuo wa Yesu Kristo kuwa bwana na mwokozi, tunakuwa watu Wake na tunapokelewa kama washirika wa kanisa Lake. Ubatizo ni mfano wa muunganiko wetu pamoja na Kristo, msamaha wa dhambi zetu, na kupokea kwetu Roho Mtakatifu. Ni kwa kuzamishwa majini na unategemea uthibitisho wa imani katika Yesu na ushahidi wa toba ya dhambi. Unafuatia mafunzo katika Maandiko Matakatifu na ukubali wa mafundisho Yake. (War. 6:1-6; Kol. 2:12, 13; Mat. 16:30-33; 22:16; 2:38; Math. 28:19, 20.)**

**16. Meza ya Bwana:**

**Meza ya Bwana ni ushirika katika mfano wa mwili na damu ya Yesu kama udhihirisho wa imani katika Yeye, Bwana na Mwokozi wetu. Katika uzoefu huu wa ushirika Kristo anakuwepo kukutana na kuwaimarisha watu Wake. Kadri tunavyoshiriki kwa furaha, tunatangaza mauti ya Bwana hadi arudipo tena. Maandalizi kwa ajili ya Meza ya Bwana hujumuisha kujihoji nafsi, toba, na ungamo. Bwana aliamuru huduma ya kutawadhana miguu kuimarishwa kutakaswa upya, kuonyesha nia ya kutumikiana wenyewe kwa wenyewe katika unyenyekevu ufafanao na wa Kristo, na kufanya mioyo yetu kuungana katika upendo. Huduma ya Meza ya Bwana ipo wazi kwa waumini wote wakristo.**
**(1 Kor. 10:16, 17; 11:23-30; Math. 26:17-30; Ufu. 3:20; Yoh. 6:48-63; 13:1-17.)**

**17. Karama za Kiroho na Huduma:**

**Mungu hukirimia washiriki wote wa kanisa Lake katika kila kizazi karama za kiroho ambazo kila mshiriki atatumia katika huduma ya upendo kwa ajili ya mema ya kawaida ya kanisa na wanadamu. Zikitolewa na uwakala wa Roho Mtakatifu, ambaye humgawia kila mshiriki kama apendavyo Mwenyewe, karama hizo hutoa uwezo wote na huduma zinazohitajiwa na kanisa katika kutekeleza shughuli zake zilizoamriwa na Mungu. Kulingana na Maandiko, karama hizi hujumuisha huduma kama imani, uponyaji, unabii, mahubiri, mafundisho, utawala, usuluhishi, huruma, na huduma ya kujitolea kwa ajili ya kusaidia na kuwatia moyo watu. Baadhi ya washiriki huitwa na Mungu na kukirimiwa na Roho kwa shughuli zinazotambuliwa na kanisa kwenye uchungaji, uinjilisti, utume, na huduma za kufundisha hasa zile zinazohitajika katika kuwapatia washiriki zana kwa ajili ya huduma, kulijenga kanisa hadi ukomavu wa kiroho, na kukuza umoja wa imani na maarifa ya Mungu. Pale washiriki wanapozitumia karama hizi za kiroho kama mawakili waaminifu wa neema mbalimbali za Mungu, kanisa hulindwa dhidi ya mivuto miharibifu ya mafundisho ya uwongo, na hukua kwa ukuaji unaotoka kwa Mungu, na hujengeka imara katika imani na upendo.**

**(War. 12:4-8; 1 Kor. 12:9-11, 27, 28; Waef. 4:8, 11-16; Mat. 6:1-7; 1 Tim. 3:1-13; 1 Petro 4:10, 11.)**

**18. Karama ya Unabii:**

**Mojawapo ya karama za Roho Mtakatifu ni unabii. Karama hii ni alama inayolitambulisha Kanisa la Masalio na ilidhihirishwa katika huduma ya Roho ya Unabii. Kama mjumbe wa Bwana, maandishi hayo ni chimbuko la Ukweli endelevu na wenye mamlaka ambao hulipatia kanisa faraja, uongozi, maelekezo, na maonyo. Pia yanaweka wazi kwamba Biblia ndiyo kipimo ambacho kutokana nacho mafundisho yote na uzoefu ni lazima vipimwe.**

**(Yoeli 2:28, 29; Mat. 2:14-21; Waebr. 1:1-3; Ufu. 12:17; 19:10.)**

**19. Sheria ya Mungu:**

**Kanuni kuu za sheria ya Mungu zimetiwa pamoja katika Amri Kumi na mfano wake ulidhihirishwa katika maisha ya Kristo. Zinadhihirisha upendo wa Mungu, mapenzi Yake, na makusudi Yake kuhusiana na mwenendo wa binadamu na mahusiano na zinawahusu watu wote katika kila kizazi. Amri hizi ndizo msingi wa Agano la Mungu na watu Wake na kipimo kwenye hukumu ya Mungu. Kupitia uwakala wa Roho Mtakatifu zinasonda dhambi na kuamsha hisia za uhitaji wa Mwokozi. Wokovu wote ni kwa neema na si kwa matendo, lakini tunda lake ni utii kwa Amri Kumi. Utii huu hukuza tabia ya Kikristo na kuleta matokeo ya hali ya ustawi. Ni ushahidi wa upendo wetu kwa Bwana na wajibu wetu kwa wanadamu wenzetu. Utii wa imani hudhihirisha uwezo wa Kristo katika kubadilisha maisha, na hivyo kuimarisha ushuhuda wa Kikristo.**

**(Kut. 20:1-17; Zab. 40:7, 8; Math. 22:36-40; Kumb. 28:1-14; Math. 5:17-20;**

**Waeb. 8:8-10; Yoh. 15:7-10; Waef. 2:8-10; 1 Yoh. 5:3; War. 8:3, 4; Zab. 19:7-14.)**

**20. Sabato:**

**Muumbaji mkarimu, baada ya siku sita za Uumbaji, alipumzika siku ya saba na kuizindua Sabato kwa ajili ya watu wote kama kumbukumbu ya Uumbaji. Amri ya nne ya sheria za Mungu zisizobadilika inaagiza utunzaji wa Sabato hii ya siku ya saba kama siku ya mapumziko, ibada, na huduma, kwa kupatana na mafundisho na uzoefu wa Yesu, aliye Bwana wa Sabato. Sabato ni siku ya mawasiliano yenye furaha na Mungu na baina yetu sisi wenyewe kwa wenyewe. Ni ishara ya ukombozi wetu katika Kristo, alama ya utakaso wetu, dalili ya utii wetu, na mwonjo wa umilele wetu wa siku zijazo katika ufalme wa Mungu. Sabato ni ishara ya daima ya Mungu ya agano Lake la milele baina Yake na watu wake. Utunzaji wenye furaha wa wakati huu mtakatifu toka jioni hata jioni, jua kucha hadi jua kuchwa ni adhimisho la matendo ya Mungu ya uumbaji na ukombozi.**

**(Mwa. 2:1-3; Kut. 20:8-11; Luka 4:16; Isa. 56:5, 6; 58:13, 14; Math. 12:1-12; Kut. 31:13-17; Eze. 20:12, 20; Kumb. 5:12-15; Waeb. 4:1-11; Walawi. 23:32; Marko 1:32.)**

**21. Uwakili:**

**Tu mawakili wa Mungu, tuliokabidhiwa na Yeye wakati, injili, fursa, afya, uwezo. Talanta, mali, na mibaraka ya dunia pamoja na rasilimali zake. Tunawajibika Kwake kwa matumizi sahihi ya vitu hivyo. Tunakiri umilikaji wa Mungu kwa njia ya kutoa huduma ya uaminifu Kwake na kwa wanadamu wenzetu, na kwa kurudisha zaka na kutoa sadaka kwa ajili ya utangazaji wa injili Yake na kwa kutegemeza ukuaji wa kanisa Lake. Uwakili ni upendeleo uliotolewa kwetu na Mungu kwa ajili ya malezi ya upendo na ushindi dhidi ya choyo na tamaa. Wakili hufurahia mibaraka inayowajia wengine kama matokeo ya uamiifu wake.**
**(Mwa. 1:26-28; 2:15; 1 Nyak. 29:14; Hagai 1:3-11; Mal. 3:8-12; 1 Cor. 9:9-14; Math. 23:23; 2 Kor. 8:1-15; War. 15:26, 27.)**

**22. Mwenendo wa Mkristo:**

**Tumeitwa kuwa watu watauwa wanaofikiri, wanaohisi, na wanaotenda kulingana na kanuni za mbinguni. Ili Roho aumbe upya ndani yetu tabia ya Bwana wetu tunapaswa kujihusisha tu katika mambo yale ambayo yatazaa usafi, afya, na furaha vifananavyo na vya Kristo, katika maisha yetu. Hii inamaanisha kwamba starehe na maburudisho yetu vinapaswa kufikia viwango vya juu vya maonjo na uzuri wa Kikristo. Huku tukitambua tofauti za kiutamaduni, mavazi yetu yanapaswa kuwa ya kawaida, ya mtindo usio wa zamani sana au wa karibuni sana, na nadhifu, yawastahilio wale ambao uzuri wao wa kweli hautokani na mwonekano wao wa nje bali ni mapambo yasiyoharibika yenye roho ya upole na utulivu. Pia inamaanisha kwamba kwa kuwa miili yetu ni mahekalu ya Roho Mtakatifu, tunapaswa**

**kuitunza kwa akili. Pamoja na kuwa na mazoezi na mapumziko ya kutosha, tunapaswa kuchagua vyakula vyenye afya zaidi kadri inavyowezekana na kuepuka vyakula vilivyo najisi, vilivyotajwa kwenye Maandiko Matakatifu. Kwa kuwa vinywaji vya vileo, tumbaku, matumizi mabaya ya madawa na madawa ya kulevya hudhuru miili yetu, yatupasa kuepukana navyo pia. Badala yake tunapaswa kujishughulisha na chochote kifanyacho mawazo na miili yetu kuwiana na Kristo, anayetamani uzima wetu, furaha yetu, na wema wetu.**
**(War. 12:1, 2; 1 Yoh. 2:6; Waef. 5:1-21; Filp. 4:8; 2 Kor. 10:5; 6:14-7:1; 1 Petro 3:1-4; 1 Kor. 6:19, 20; 10:31; Lawi. 11:1-47; 3 Yoh. 2.)**

**23. Ndoa na Familia:**

**Ndoa ilizinduliwa na Mungu kule Edeni na kuthibitishwa na Yesu kuwa ni muunganiko wa maisha yote baina ya mwanaume na mwanamke walio katika mahusiano ya upendo. Kwa wakristo, kifungo cha ndoa ni kwa Mungu na baina yao wenyewe kwa wenyewe na inapaswa kuingiwa tu baina ya washirika wawili walio kwenye imani moja. Kupendana, kuheshimiana, kustahiana ni nyuzi nyuzi za mahusiano haya, zinazopaswa kuakisi upendo, utakatifu, ukaribu na udumishwaji wa mahusiano baina ya Kristo na kanisa lake. Kuhusu talaka, Yesu alifundisha kwamba mtu amwachaye mwenzi isipokuwa kwa sababu ya uasherati na akaoa au kuolewa na mwingine azini. Ingawaje baadhi ya mahusiamo ya kifamilia yaweza kushindwa kufikia viwango, wenzi katika ndoa ambao wamejitoa kikamilifu kila mmoja kwa mwezake katika Kristo wanaweza kufikia umoja wenye upendo kupitia uongozi wa Roho na malezi ya kanisa. Mungu hubariki familia na hukusudia kwamba wanafamilia wasaidiane wao kwa wao kufikia ukomavu mkamilifu. Wazazi wawalee watoto wao katika kumpenda na kumtii Bwana. Kwa kielelezo chao na maneno yao wawafundishe kwamba Kristo ni mtiishaji mweye upendo, daima mpole na mweye kujali, anayetaka wawe viungo vya mwili wake, familia ya Mungu. Ukaribu wa kifamilia unaoongezeka ni mojawapo ya alama za ujumbe wa mwisho wa injili.**
**(Mwa. 2:18-25; Math. 19:3-9; Yoh. 2:1-11; 2 Kor. 6:14; Efe. 5:21-33; Math. 5:31, 32; Marko. 10:11, 12; Luka. 16:18; 1 Kor. 7:10, 11; Kut. 20:12; Waeb. 6:1-4; Kumb. 6:5-9; Mith. 22:6; Mal. 4:5, 6.)**

**24. Huduma ya Kristo katika hekalu la mbinguni:**

**Kuna hekalu mbinguni, hema la kweli lililosimamishwa na Bwana na siyo mwanadamu. Ndani yake Kristo anahudumu kwa niaba yetu, akiwezesha kupatikana kwa ajili ya waumini fanaka za kafara Yake ya upatanisho iliyotolewa mara moja msalabani kwa ajili ya wote. Alizinduliwa kuwa Kuhai wetu Mkuu na akaanza huduma Yake ya uombezi wakati wa kupaa Kwake mbinguni. Mnamo mwaka 1844, mwishoni mwa kipindi cha unabii wa siku 2,300, aliingia katika awamu ya pili na ya mwisho ya huduma Yake ya upatanisho. Ni kazi ya hukumu ya upelelezi ambayo ni sehemu ya mwisho ya huduma yake ya upatanisho. Ni kazi ya hukumu**

**ya upelelezi ambayo hatimaye itakomesha dhambi yote, iliyokuwa mfano wa kutakaswa kwa hekalu la kale la Waebrania katika Siku ya Upatanisho. Katika huduma hiyo kielelezo hekalu lilitakaswa kwa damu ya wanyama wa kafara, lakini mambo ya mbiguni hutakaswa kwa kafara kamilifu ya damu ya Yesu. Hukumu ya upelelezi hufunua kwa viumbe wa mbinguni ni nani miongoni mwa wafu wamelala katika Kristo na hivyo, katika Yeye wanahesabiwa kustahili kuwa na sehemu katika ufufuo wa kwanza. Pia inadhihirisha wazi ni nani miongoni mwao walio hai wanakaa ndani ya Kristo, wakiishika Amri za Mungu na imani ya Yesu, na katika Yeye hivyo basi, wako tayari kwa kuhamishwa kuingia katika ufalme wake wa milele. Hukumu hii huthibitisha haki ya Mungu katika kuwaokoa wale wanaomwamini Yesu. Hutangazwa kwamba wale waliodumu kuwa watiifu kwa Mungu watapokea ufalme. Hitimisho la huduma hii ya Kristo itakuwa ndiyo mwisho wa kufungwa kwa mlango wa rehema ya wanadamu kabla ya Marejeo ya Yesu.**
**(Waeb. 8:1-5; 4:14-16; 9:11-28; 10:19-22; 1:3; 2:16, 17; Dan. 7:9-27; 8:13, 14; 9:24-27; Hes. 14:34; Eze. 4:6; Law. 16; Uf. 14:6, 7; 20:12; 14:12; 22:12.)**

**25. Kuja kwa Kristo mara ya pili:**
**Kuja kwa Kristo mara ya pili ndilo tumaini lenye baraka la kanisa, hitimisho kuu la Injili. Kuja kwa Mwokozi kutakuwa halisi, binafsi, kutakakoonekana, na kwa dunia nzima. Atakaporudi wenye haki waliokufa watafufuliwa na pamoja na wenye haki walio hai watavikwa utukufu na kuchukuliwa kwenda mbinguni, lakini waovu watakufa. Kutimizwa karibu kabisa kwa sehemu nyigi za unabii, pamoja na hali ya sasa ya ulimwengu, huonyesha kwamba kuja kwa Kristo ku karibu sana. Wakati wa tukio hilo haukufafanuliwa, na hivyo basi tunahimizwa kuwa tayari kwa nyakati zote.**
**(Tito 2:13; Waeb. 9:28; Yoh. 14:1-3; Mat.1:9-11; Math. 24:14; Uf. 1:7; Math. 24:43, 44; 1 Thess. 4:13-18; 1 Kor. 15:51-54; 2 Thess. 1:7-10; 2:8; Uf. 14:14-20; 19:11-21; Math. 24; Marko13; Luka 21; 2 Tim. 3:1-5; 1 Thess. 5:1-6.)**

**<u>26. Mauti na Ufufuo:</u>**
**Mshahara wa dhambi ni mauti. Lakini Mungu ambaye peke yake hapatikani na mauti, atawapa uzima wa milele waliokombolewa Wake. Mpaka siku hiyo mauti ni hali ya kutokuwa na fahamu kwa watu wote. Wakati Kristo aliye uzima wetu, atakapotokea, wenye haki waliofufuliwa na wenye haki walio hai watavikwa utukufu na kunyakuliwa juu ili kumlaki Bwana wao. Ufufuo wa pili ambao ni ufufuo wa waovu, utatokea miaka elfu moja baadaye.**
**(War. 6:23; 1 Tim. 6:15, 16; Maomb. 9:5, 6; Ps. 146:3, 4; Yoh. 11:11-14; Kol. 3:4; 1 Kor. 15:51-54; 1 Thess. 4:13-17; Yoh. 5:28, 29; Uf. 20:1-10.)**

**<u>27. Miaka elfu moja na mwisho wa dhambi:</u>**
**Milenia ni miaka elfu moja ya utawala wa Kristo pamoja na watakatifu Wake mbinguni kati ya ufufuo wa kwanza na wa pili. Wakati huo waovu**

**waliokufa watahukumiwa; dunia itakuwa ukiwa na utupu, bila wanadamu wakazi walio hai, lakini ikikaliwa na shetani na malaika zake. Mwishowe Kristo na watakatifu Wake na mji Mtakatifu, watashuka duniani kutoka mbinguni. Ndipo waovu waliokufa watafufuliwa, nao pamoja na shetani na malaika zake watauzigira mji; lakini moto kutoka kwa Mugu utawateketeza na kuitakasa dunia. Na Na hivyo ulimwengu utakuwa huru bila dhambi na weye dhambi milele.**
**(Uf. 20; 1 Kor. 6:2, 3; Yer. 4:23-26; Uf. 21:1-5; Mal. 4:1; Eze. 28:18, 19.)**

**28.Nchi Mpya:**

**Katika dunia mpya, ambamo haki hukaa, Mungu ataweka tayari makao ya milele kwa waliokombolewa na mazingira makamilifu kwa maisha ya milele, upendo, furaha, na kujifunza mbele Yake. Kwa kuwa hapa Mungu mwenyewe atakaa pamoja na watu wake, na taabu na mauti zitakuwa zimepita. Pambano litakuwa limemalizika, na dhambi haitakuwepo tena. Vitu vyote vyenye uhai na visivyo na uhai vitatangaza kwamba Mungu ni Pendo; Naye atatawala milele. Amina.**
**(2 Petro 3:13; Isa. 35; 65:17-25; Math. 5:5; Uf. 21:1-7; 22:1-5; 11:15.)**

**ALFABETI ZA MALEZI YA WATOTO au mzazi wa karne ya 21 au nini? Najaribu kutoa Machache, kitabu hiki kipo mtandaoni bure**

1. (The main thing, is to keep the main thing, the main thing)
JAMBO MUHIMU NI KUFANYA, JAMBO MUHIMU KUWA JAMBO MUHIMU
2. MTOTO AKIWA TUMBONI MWA MAMA
3. HATUA ZA KUKUA ZA MTOTO
4.WATOTO KATIKA BIBLIA
5.MAZIWA YA NG'OMBE AU MAZIWA YA MAMA
6. MTOTO SHULENI
7 KWANINI MUNGU ALITUPATIA WATOTO
8 UGUMU WA KAZI YA UZAZI
9 ELIMU YA NGONO KWA VIJANA
10. MAOMBI YA NYUMBANI (IBADA)
11. TARATIBU NYINGINE ZA NYUMBANI
12. MAWASILIANO NA WATOTO
13. NDOA TAKATIFU
14. TALAKA NA MATOKEO YAKE
15. MABIBI NA MABABU NA WALEZI WENGINE
16. KUWEKA VIWANGO KWENYE FAMILIA (FAMILY VALUES)
17 . WATOTO AMBAO NI WATU WAZIMA
18. KUKATA KITOVU CHA MTOTO
19. WATOTO AMBAO NI WATU WAZIMA NA WANAISHI NYUMBAN
20. AFYA YA WATOTO
21. WAKWE NA WAZAZI WENZA (afya)
22. BABA NA MALEZI YA WATOTO
23. MAMA NA MALEZI YA WATOTO
24. KUCHAGUA MWENZI WA MAISHA
25. BURUDANI, MICHEZO, NA MARAFIKI
26. MAGONJWA YALETWAYO NA FASHENI (IKKCW)
27. KUADABISHA
28. UMASIKINI NA MAZINGIRA MAGUMU YA MTOTO
29. KUSAIDIA KAZI, KUHUDUMIA NA KUFUNDISHA USTADI NA UJASILIAMALI
30. UNYANYASAJI WATOTO (IKKCW)
31. MUZIKI, UCHAWI NA MENGINEYO
32. WATOTO NA VYOMBO VYA HABARI NA TEKNOLOJIA (IKKCW)
33. WAZAZI SOLEMBA (Single parenting).
34. KUFUNDISHA, WATOTO NYUMBANI
35. MIFANO YA KAZI AMBAZO UNAWEZA KUWAPA WATOTO KUTOKANA NA UMRI
36. NENO LA MUNGU
37. MAOMBI )
38. a. MAMBO zaidi ya 101, TUNASHAURI UFANYE NA WATOTO WAKO
b. Mambo 20 yanayosaidia Tabia njema kwa watoto
39. AFYA YA wazazi

41. KUKUZA MTOTO WA KIUME AWE KIONGOZI
42. KUKUZA MTOTO WA KIKE KUTOKANA NA MITHALI 31 (IKKCW)
43. HITIMISHO LA JAMBO MUHIMU LA MALEZI YA WAZAZI.

A. Maswali na majibu ya wazazi au watoto

B. Dondoo za Huduma mbali mbali

**KUKUZA MTOTO WA KIUME AWE KUHANI KUSIMAMIA NYUMBA YAKE au**
**(kukuza mwana awe mlei- wameandikiwa watoto wa kiume na wazazi**

**Wengi wameandika vitabu vya kukuza watoto wa kiume kwa waumini. Kukuza mtoto wa kike hakuna tofauti kubwa na kukuza mtoto wa kiume isipokuwa pale majukumu ya jinsia yanapotofautiana, kama vile ambavyo Mungu alituagiza. Mungu Ndiye mzazi mkubwa, Maandiko ndiyo kitabu cha malezi kikubwa, vingine ni kujazia hicho. Jambo kubwa la kuwasaidia watoto wetu, ni kuwafanya waweze kuishi bila sisi. Waweze kukabiliana maisha kwa mahusiano na Mungu, jumuiya yaani shuleni au kazini, ushirika, na familia zao.**

1. ***Mbingu na dunia ndiyo vitabu vya mtoto wa kiume, kabla hajaanza kujua kusoma au kuandika, kama Zaburi 19 inavyosema. Zaburi 144: 12-15 yasema, 'Wana wetu na wawe kama miche waliokua ujanani. Binti zetu kama nguzo za pembeni zilizonakishiwa kwa kupamba hekalu. Ghala zetu na zijae akiba za jinsi zote. Kondoo zetu na wazae elfu na makumi elfu, mashambani mwetu ngombe zetu na wachukue mizigo, kusiwe kushambuliwa. Wala kusiwe kuhamishwa. Wala malalamiko katika njia zetu. Heri watu wenye hali hiyo. Heri watu wenye Bwana kuwa Mungu wao."***

Tafsiri ya Mungu ya mwanamume ni zaidi ya kuonekana kwa nje; maana Ezekieli 22:30 yatuambia, ni mtu atakayekuwa tayari kutengeneza pale palipobomoka. Kuwa mwanamume katika Neno la Mungu ina maana kiroho, kiakili, kihisia na kimwili. Mtoto anasaidiwa nyumbani, kwenye jumuiya, shuleni na kanisani kukua ipasavo.

**Baada ya kupata watoto lazima tuwe na mipango maana Mungu ametupa wana kama mawakili, ni bustani yetu kupalilia, mpaka wakue na kukomaa. Hatuwezi kukaa tu na kufikiri mambo yatajipa yenyewe. Chakula na nguo havitoshi kukamilisha malezi ya watoto.**

**Watoto wetu wa kiume watakuwa viongozi katika jumuiya zao, watakuwa makuhani kwenye nyumba zao na watakuwa kaka zetu kule mbinguni siku moja. Tunamtayarisha mtoto wetu wa kiume kuwa mume, baba na muumini katika nyumba ya Mungu. Hii ni safari inayohitaji muda mwingi, na imekita kwenye mhimili wa Neno la Mungu.**

**Neno la Mungu ndiyo mwanzo na mwisho katika malezi (alfa na omega). Neno la Mungu ndiyo usalama wetu pekee wazazi na watoto**

**wetu. Hebu uweze kuvuna matunda ya kazi yako, ya uaminifu kwa Mungu; na uweze kuwasaidia watoto wako kuwa mashujaa, wanaochukua majukumu na kuzaa matunda mengi ya haki. Luka 2:52 yasema, Yesu alikua kwa kimo na hekima akimpendeza Mungu na wanadamu. Miaka ya kumi na, (teenage), si lazima iwe na shida za ujana na uasi, bali ya uzalishaji (productivity) kwa mwana, wazazi na jumuia. Tusichoke kutenda mema. Maana siku moja 'baba yako na mama yako watafurahi , na yeye aliyekuzaa atashangilia'. 'Sisi kama wazazi tuwachukue watoto wetu kwenye semina za injili au walei, tusiwaache. Tuwachukue katika shughuli tunazomfanyia BWANA ili wajifunze kwa matendo na kuipenda kazi Yake BWANA.**

**Kukuza mtoto wa kiume ampendaye Mungu yahitaji kuwajibika (commitment), maana watoto wetu wa kiume siku hizi wana changamoto ya kujishughulisha kwa bidii, kwenye taaluma na hata kazi za mikono. Asilimia 90% ya mashamba Afrika hulimwa na wakina mama watu wazima. Pia Asilimia 80 ya waumini wengi kwenye nyumba za ibada ni wana wa kike, na ndiyo waonekana na hari ya kwenda shule na kusoma vitabu kwenye nchi nyingi. Zamani kuna masomo kama hisabati au fizikia yaliaminika kuwa masomo ya kiume; na watoto wa kiume ndio walichukua maksi za juu. Utafiti wa Dr Nedley Marekani unasema kwamba namba hizi zataka kufanana na za watoto wa kike siku hizi. Akaongeza kwamba watoto wa kiume wanaona hakuna haja ya kujishughulisha siku hizi kwani kupata mke wa kuoa ni rahisi, wala uhitaji mahari kama zamani.**

**Wasichana siku hizi ndio wanafuata wavulana. Hii inawafanya wasiwajibike au wasione changamoto au ari ya kufuatilia kitu. Anasema pia watoto wengi wa kiume wanaweza kumudu maisha yao wakitegemea wazazi au mke mpaka uzeeni, endapo mke atashtuka na kumwacha, mke huyu atachukua watoto aende nao, na mume atarudi kwa wazazi na kuwategemea.**

**Mtoto wa kiume ameumbwa kwa mfano wa Mungu naye aliumbwa kabla ya mwanamke. Kusudi lake duniani halikuwa kuongeza na kujaza nchi kwanza, bali kumpa Mungu utukufu na kumiliki na kutiisha nchi. Wana wetu ni lazima wajue hili kwanza. Mtoto wa kiume alipewa kazi ya bustani hata kabla ya maanguko ya binadamu. Utii kwa Mungu na mzazi, ndiyo somo la kwanza kwa wana wetu. kisha mipangilio,Ustadi, taaluma, kutawala nafsi, na kazi za mikono. Hivi vinamsaidia kukana nafsi na kutawala nafsi na kuitafutia riziki familia. Zamani mtoto wa kiume Afrika ndiye aliyetunza wazazi, na kutegemewa na dada zake au wadogo zake kama ndiye mtafutaji, mshauri na kiongozi. Jambo hili limeanza kupungua kwa kiasi fulani.**

**Japo hiyo ni takwimu ya Marekani, ila unapoona mwenzako ananyolewa, wewe anza kutia maji kichwani. Nchi hii ya Marekani inaweka viwango mara nyingi, japo ni vibaya kama vile vya ushoga, lakini watu wengine wanavifuatilia kirahisi. Mengi siku hizi watoto wanayoona kwenye vyombo vya habari, hasa runinga, yanaigizwa na vyombo hivi vyawa kama mzazi. Hii ni hatari maana vyombo vingi vya habari, vina machache mazuri, hata kwenye matangazo, watu wanavyozungumza na**

**kuvaa kunakuwa na walakini fulani.**

**Nilipokuwa mtoto, ilikuwa matusi kumwita mvulana 'msichana;' ila siku hizi hata wavulana wenye nguvu na akili wameingia desturi za maovu kama ushoga, jambo ambalo lilikuwa mwiko, hata kwa wale wasiomcha Mungu. Watu wa nchi kama Ufilipino wanasemekana wanaongoza katika takwimu ya kufanya upasuaji wa wanaume kujibadilisha kuwa wanawake ili maisha yao 'yawe rahisi'. Hii ni kutojua kwamba katika uumbaji, mwanamume ndiye alitangulia kuumbwa, naye ni kichwa, na anapaswa kuheshimiwa na mwanamke. Na hata hivyo mwanamke ni mfanya dhambi wa kwanza na sidhani kama hilo linavutia mtu ye yote.**

**Herodi aliua watoto wa kiume. Farao pia, alijua akimaliza watoto wa kiume, basi taifa limekwisha. Hata Balaam aliangusha wanaume 24,000 wa Israeli, akijua akimaliza hao amemaliza taifa. Mungu amempa mtoto wa kiume na wanaume karama na jukumu ambalo wana wa kike hawakupewa, hivyo tunapokuza watoto wa kiume tuangalie hili. Wakina baba wakae na watoto wa kiume na kuwafundisha kwa matendo. Wanasema wakina baba wengi hukaa pungufu ya dakika nne kwa siku kuzungumza na watoto wao.**

**Yapasa kuwa na uchaguzi wa mambo mengi kama vile marafiki, miziki tunayosikiliza, vitabu tunavyosoma, elimu tunayopata, kanisa tunalohudhuria, nguo tunazovaa, na mengine mengi. Wazazi tusome Neno la Mungu ili tupate majibu, na viwango vinavyofaa, pia tujifunze kuwa waumini waliokomaa, na kuhudumu pamoja. Hata wale wazazi solemba wanaweza kukuza watoto wanaompenda Mungu. Tunaona Timotheo, na bibi yake Loisi na mama yake Yunia, wakimsaidia Timotheo kuwa shujaa aliyehudumu wengi kama mlei na kisha mchungaji.**

**Lazima uwe na malengo na mipango ya mwaka mmoja. Huwezi ukafanya yote kwa pamoja, weka ramani kidogo, kile unachotaka ukipate, usilinge gizani ili watoto wahitimu toka nyumbani. Watoto wakiwa wadogo wanakuwa kama taulo/sponge; inayonyonya maji mengi. Wanashika mengi ya sayansi na kukariri sana. Tumia muda huu kuwafundisha kutoka kitabu cha viasili/uumbaji na dunia. Mafundisho ya 1 Wakorintho 13 ya upendo, ni muhimu kwa watoto na sisi.**

**Daima watoto wetu wafundishwe uumbaji wa Mungu na si uibukaji, (evolution). Hili tulipatie kipaumblele; 1 Kor 3:19. Tutumie msaada wa mababu na mabibi kuwasaidia watoto.**

**Watoto wafundishwe kujenga nyumba, kushona, kupika, kulima na ustadi mwingine. Wafundishe watoto kuzungumza kwenye umma, kupanga muda wao, na kutathmini wanavyoendelea. Furahi nao kwa walichokiwezea. Wafundishe mashujaa wa mifano ya Neno la Mungu kama Daudi, Nuhu au Ibrahimu. Mwulize kijana wako mashujaa wake ni wapi? Ni watu wa filamu au michezo ya Kompyuta? Je, awezaje kuwa mshumaa au mwanga wa nyumba yake?**

**Soma vitabu kama '10 Boys Who Changed the World,' kilichoandikwa na Irene Howard. Je, anawahusudu (admire) watu ambao hawampendi Mungu kama Samsoni alivyowapenda Wafilisti? Je, anasoma vitabu vya namna gani?**

**Maisha ya mwanamume yamejaa maamuzi mbali mbali, na kutenda**

**kutokana na maamuzi, tuwatayarishe vijana wetu kuchukua majukumu kwa kuamua mambo inavyotakiwa. Watayarishe vyema kisha waachiwe nafasi wafanye maamuzi, na wanapokosea wajue kusahihisha. Jifunzeni hata toka kwa wadudu kama siafu, na mifano ya watu kama ya kijana Yusufu, Yethro, Abigaili, Msamaria mwema, Boazi na wengineo.**

**Usipokuwapo anafanya shuguli vyema? Je, anasalimu watu?, anafanya kazi za nyumbani? Angalia kama anatumia muda wake vizuri, na kuacha vitu vyake katika mpangilio na usafi. Je, anajua kutatua matatizo, au anasahau majukumu yake? Je, anajua muda ni mali na hasemi nitafanya kesho?**

**Mpeleke polisi, au kotini kutokana na umri na kisha mjadili kesi za kawaida mnazoruhusiwa kuhudhuria. Soma visa kama vya Akani na Samsoni mjadili. Je, apenda kutoa udhuru au kutia chumvi, na kuweka ahadi asizotimiza? Je, anachukua vitu vya watu bila ruhusa? Je, anapenda umbeya na kushuhudia watu uongo? Tusiwakinge sana watoto wetu na maumivu au kushindwa. Mara nyingine ni lazima washindwe ili wajifunze, ila wasiwe na woga wa kujaribu tena. Soma habari za mashujaa 30 wa Daudi (1 Mambo ya Nyakati 11). Pia soma kuhusu mashujaa wa matengenezo kama Luther, Zwingli, Tyndale, Knox, na Huss. Je, aweza kukubali kukosolewa na ajifunze? Je, ana ujasiri wa kujua amefanya dhambi akatubu na kuiacha? Je, anaweza kusema amekosa na kuungama? Je, anaogopa watu zaidi ya Mungu?**

**Mwanamume ni kichwa cha familia, kama vile Kristo alivyo kichwa cha kanisa, angalia tabia za wanaume kama Nuhu, Ayubu, Ibrahimu, Musa, Daudi. Ibrahimu shujaa alisifiwa, 'Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe na nyumba yake baada yake waishike njia ya BWANA wafanye haki na hukumu.' Mtoto wa kiume yapaswa ajue mafundisho makuu ya imani kwa uhakika na kutofautisha mafundisho ya uongo-(doctrines). Maana atakuwa kuhani wa mji wake, na hata nyumba ya ibada. Awahoji wachungaji na viongozi wa kiroho vile wanavyoamini. Je, injili ni nini? Inawaathirije maisha yao? Kumbukumbu 6:7,8 wafundishwe watoto na wakariri. Wazazi wasaidie watoto wa kiume kuwa walimu.**

**Kujifunza uongozi ni muhimu. 1 wafalme 3:9; 'Nipe mimi mtumwa wako moyo wa adili niwahukumu watu wako, na kuwapambanua mema na mabaya, maana ni nani awezaye kuwahukumu hawa watu wako walio wengi?' Hapa Sulemani aliomba hekima na uongozi. Twatoa mifano kwa wana wetu kuwa mahakimu wa haki. Tunapowaadabisha, tunainua sheria ya Mungu, na kuwasaidia katika mausia ya Bwana. Twafundisha kuzungumza na marafiki zao wanapowakosea, ili kuweza kurudisha uhusiano mwema, kusudi waweze kuwasaidia watoto wao wanapofanya makosa ya sheria ya Mungu. Hakikisha adhabu zako kwa mtoto zinalingana na upendo wako, endapo adhabu zako zinazidi upendo kuna walakini. Twasema vile tukijua wote ni binadamu tunakosea, na kila mtu ana mizoga fulani katika shuguli ya kulea, ila adhabu iwe ya upendo, kumrudi mtoto, na si hasira. Usimpe mtoto adhabu ukiwa na hasira, ngoja ipoe, kisha uzungumze naye, na kisha umpe adhabu. Ajue alichokosea, na**

**ajue jinsi ya akusahihishe.**

**Je, mtoto aweza kuwaongoza wengine kwa unyenyekevu na kugawa kazi, hata kuzisahahisha na kutathmini? Angalia "Brother Offender Checklist" na "21 Rules of This House" kwenye website ya maneno hayo. Muwe na koti nyumbani, ili muamue lipi lahitaji adhabu na lipi lahitaji maonyo. Angalia kwenye maandiko adhabu za manabii, za watu na za mitume. Orodhesha dhambi ambayo mtoto anapambana nayo, panga adhabu, na matokeo ya kukataa maonyo. Je! mamlaka yana majukumu gani, tunapaswa tutendeeje mamlaka. Je! mwana wako anakubali kufundisha wengine, kama darasa la watoto au vijana wenzake kanisani?**

**Mtoto wa kiume afundishwe kutokuwa na tamaa ya vitu vya mtu, na kushukuru kwa alivyo navyo, kwa maana Utauwa na kuridhika ni baraka kubwa, kwani tulikuja duniani bila kitu na tutaondoka bila kitu. Pale anapokosea afundishwe kuomba msamaha. Kwa vile atakuwa kiongozi afundishwe kutumia mamlaka na majukumu kwa hekima. Mfano wa waliotumia madaraka vibaya ni mafarisayo, na waliotumia madaraka vizuri ni Nuhu, Ayubu Eliya, n.k. Ajue kwamba madaraka ni kuwa mhudumu au mtumishi wa watu na wala si dikteta wa kunyanyasa watu. Ajue kufanya kazi kwa mikono yake ili aweze kukidhi mahitaji yake na ya wengine. Apaswa kuanza kufunga na kuomba akifika miaka kumi na miwili hivi, maana mengi hayawezekani pasipo maombi na kufunga. Ajue kwamba mke na watoto wake watahitaji nguo, chakula na makazi na hivi ni sababu tosha ya yeye kujifunza kusali na kufunga.**

**Ukengeufu au upotofu waanza pole pole, kama vile kipima joto kinavyoongezeka; hivyo agundue kwamba baada ya muda atajikuta mbali. Ajifunze kutoka kwa wanaume wenye hekima na wenye tabia njema, maana wanaume hawa wamepitia maisha ya ushindi na maanguko, ili asikanyage pabaya, na kudidimia. Majaribu yanaonekana mazuri, ila hayasemi ukweli wote, asijaribu kupambana na majaribu bali amwuulize Mungu kutii na kuepuka mialiko ya kufanya uovu, kwani pambano ni la Mungu unapochagua, kutii sheria Yake.**

**Kwa nini ni vizuri kijana asijihusishe na nyimbo kama za Rock muziki na za dansi? Kwa sababu zina uovu, watu wengi wanaoimba wanapendelea uasi wa sheria za Mungu, na kujiingiza kwenye dini za kuabudu miungu mingine zaidi ya Mungu wa Ibrahimu, wanajishughulisha na vileo au madawa ya kulewa, wanafundisha mambo ya giza bila kujua na pia wanafanya mionjo ya kiroho ipungue, wakiongeza wasiwasi na kutotulia kwa moyo.**

**Elimu ni nzuri ila, anza kusoma vitabu mapema, kabla mambo hayajaribika. Mweleze kijana pia. Yaani asisome kitabu cha kuwa na ndoa nzuri baada ya kuachana na mke, ila kabla. Kuelimika na kusoma ni vitu viwili tofauti, unaweza kusomea shahada kubwa ila usielimike. Na pia kupata pesa na kufanya kazi ni vitu tofauti. Neno la Mungu limehakikishwa kwa kila hali ili lisaidie kwa mafundisho, kuonya makosa, kuongoza, kuadabisha kwa haki, ili mtu awe kamili na apate kutenda kila tendo jema.**

Mtoto ajifunze kutii utawala, maana hata yeye siku moja aweza kuwa kwenye shuguli ya uongozi. Huwezi kuongoza watu kama wewe hujui kuwa mfuasi. Tunaambiwa katika Maandiko matakatifu kwamba tuwaheshimu na kuwatii wanaotuongoza, ili kazi yao isiwe ngumu au ya huzuni, maana watatoa hesabu kwa yale wanayofanya. Angalia tu shuguli ambazo serikali ya kawaida inasaidia raia. Tunaelewa kwamba tuna viongozi waovu, ila kwa kawaida viongozi ni msaada mkubwa na hatuwezi kamwe kuishi bila viongozi. Endapo wazazi tunafanya kazi ya viongozi kuwa ngumu au tunawadharau, watoto wataiga.

Kusamehe ni muhimu kwa mtoto wa kiume, na kutosamehe ni kama kunywa sumu na kutegemea mwingine afe.  Na pia tukumbuke hata sisi tumewakosea wengine na wanatusamehe. Wapaswa kuwa huru kwa aliyekukosea na si mtumwa wake. Hata hivyo tunasamehewa tunavyosamehe.

Mwana ajifunze kusamehe, na kumwambia Mungu uchungu alio nao, na kumwomba aondoe uchungu huu, asiseme uongo bali kweli ya moyoni kwa Mungu, kwani  BWANA anao uwezo wa kutoa uchungu na chuki yote, na atashangaa moyo wake utakuwa mwepesi. Mke, watoto na hata wazazi wanaweza kumkosea. Ila twapasa kujua jinsi ya kutatua haya matatizo, kwani tumeambiwa kwamba ni vyombo dhaifu, hivyo twahitaji hekima ya kuenenda nao. Ajifunze kumwachia Mwenyezi Mungu shida yake hiyo, na ikirudi mawazoni amwachie tena, mpaka itoke kabisa.

Kuweka visasi na chuki ni kitu cha kuangamiza kabisa, Je, tunawezaje kutoa mawazo machafu? Mawazo machafu yanakuja kwa kila binadamu Je, tunayaondoaje? Wengi wanakosa kujikana nafsi na kuzungumza lolote, kuwaza au kutenda chochote. Je, ana  hasira anayoshindwa kuikabili?  Au mawazo mabaya? Zaburi 119:110 yasema, tuweke Neno Lake mioyoni mwetu ili tuondoe mawazo machafu, kisha kama Yoshua, tuchague nani tutamtumikia kila siku. Tuchague kumtumikia Mwenyezi, Naye atatuondolea mawazo machafu. Mawazo yetu lazima 'Tuyaangushe na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mwenyezi Mungu, na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii BWANA; 2Kor 10:5. na hatimaye, mwishowe tufikirie yote mazuri, ya ripoti njema na ya staha.

Udadisi wa mtoto uweze kukuzwa ili aweze kubuni na  kuvumbua mambo. Mpe mtoto vifaa na muda, usiwe unajali sana  kwamba ataharibu vitu, au anapoteza muda. Watu waliovumbua duniani walihitaji  muda, watu wanahitaji uwaamini na kutokuwa na presha au misukumo mingi. Ili mtoto aweze kuvumbua anahitaji maarifa katika masomo tofauti. Mungu Ndiye mvumbuzi mkubwa, usipoteze muda wako kuvumbua uovu utakaongamiza watu kama wale waliovumbua mabomu ya nuklia! Jaribu kuwa na vitu vigumu visivyoharibika haraka, vigumu na vichache!

Kitu kikubwa katika uvumbuzi ni kutokata tamaa. Thomas Edison alifanya majaribio 1,000 yaliyoshindwa ila alivumbua taa na mengineyo. Aligundua njia 1,000 za kutofanya majaribio kwa njia hizo  (1,000 ways not to go). Usikate tamaa ushindwapo, jifunze kutokana na makosa na usonge mbele, utapata majibu.

Mtoto wa kiume ameumbwa avumbue nyimbo, program, vitu, mbinu,

sanaa, vitabu, zana, na mengineyo. Hebu uwe mvumbuzi kama Mungu alivyokupangia, kuhudumia dunia, na kuishi maisha yenye maana. Ila usisahau afya ya mwili wako kwa kufanya mazoezi ili usiwe lege lege ukikaa kwenye maabara siku nzima bila kuona jua, na kupata hewa bora!

Mtoto wa kiume, ajifunze kuvumilia, na ajifunze kutunza urafiki. Asiwe mtu wa kukasirika ovyo ovyo na kushindwa kukarabati urafiki. Mara nyingi kama binadamu tunashindwa mengi, ila ujasiri na kujaribu tena na tena ni muhimu. Tunaona hata Mungu hatuachi tunaposhindwa na bado anakarabati maanguko yetu yaliyotokea kwenye bustani ya Edeni, Mwanzo 3. Toka sura ya 4 ya Mwanzo mpaka leo ukarabati unaendelea.

Je, napaswa niwe wapi (belong)? Mara nyingine unaweza kuona kwamba haufai kuwa mahali fulani. Kwa kweli mbinguni ndiko kwetu sisi wote, huko ndiko tutapoona ni maskani yetu kamili. Usipoteze muda mwingi kuona kama unafit hapa, maana Mwenyezi ameenda kututayarishia makao, na hivyo mara nyingi tutajisikia tu wageni hapa, ila tuweke nia na shabaha yetu kwenye ile nchi ya Paradiso. Afadhali kuishi kama mgeni hapa ukijitayarisha kwenda mbinguni, kuliko ujisikie mwenyeji na mwishowe ulie na kusaga meno. Tutakapolenga mbingu, hata ya dunia itakuwa rahisi kuyakabili, ila tukilenga dunia tu, tutakosa mengi.

Kutenda haki ni muhimu la sivyo mvulana anakuwa mtumwa wa tamaa zake na kutojikana nafsi. Kutendea watu wote haki ni muhimu, na pia kuwiwa na upendo na watu. Twaona mfalme Sulemani alihukumu kwa haki, ila alipoanza kutojikana nafsi, kwa kuchukua wake wengi, alipoteza haki za watu, na kuharibu mahusiano na Mungu. Mara zingine vijana wa kiume wanafikiri haya hayawezi kuwapata wao. Wanasema tukifikiria kwamba haya hayawezi kutupata, basi tu wenye hekima kumzidi Sulemani, wenye nguvu kumpita Samsoni, na tunampenda Mungu kuliko Daudi.

Maisha ni kufanya kazi, kusoma, kujenga, kuwekeza, usiwe mvivu na kukaa tu. Usikae kivivu kijiweni (jobless corner) mpaka nguo kuchanika kwenye makalio, huo si mpango wa Mungu kwa mvulana. Msichana aweza kuolewa na mtu mwenye uwezo, wewe mvulana ndiyo mtafutaji. Ni aibu kunyemelea msichana tajiri eti maisha yako yawe rahisi. Kama ni mipango ya Mungu itokee vile, basi nawe ujishughulishe na kuwa mtafutaji ili usidharauliwe na mke au wakwe zako. Kama unataka kuwa injinia, lazima usomee hesabu na sayansi kuanzia leo. Kama unataka kuwa kuhani, anza kupanga mikakati wa kusoma Maagizo ya Mungu. Mungu ametuumba kuwa watendaji na si watazamaji.

Jifunze kusoma Neno la Mungu, ukiamka tu, goli si kwamba umesoma kurasa ngapi, bali mahusiano yako na Mungu. Mungu anataka kuzungumza yale ya muhimu kwako (concerns), anataka ajue ndoto zako. Mungu ana nguvu tosha za kumwamsha mwanamume au mvulana mnyonge atoke kwenye kitanda na kusoma Neno lake, mwombe akusaidie uamke na kusoma. Mwumbaji ataka awe karibu nawe, hebu mruhusu.

Mara nyingi katika maisha watu watashindwa kutuelewa. Kutoeleweka kwingine (misunderstood), kama umesingiziwa, jifunze kukaba ulimi wako na kusema kweli tu mpaka yale uliyosingiziwa yapite. Ila kusingiziwa ni nafasi ya Mungu kutufundisha uvumilivu, unyenyekevu

na kusamehe watu. Hata Bwana alisingiziwa na kusemewa uongo. Badala ya kukasirika na kushangaa, poa na umwombe BWANA nguvu. Uwe na amani moyoni, kwamba Mungu anaelewa, na kujua nia yako ya ndani. Kutenda mema ni silaha. Mwenyezi anatumia kupinga yale ambayo watu wanayotusingizia au kukupachika.

Mara nyingine hutaelewa na utachoka kusingiziwa na kueleweka visivyo, ila kumbuka tuko katika pambano kuu kati ya wema na ubaya. Shetani amemsingizia Mungu kwamba hatendi haki, na wengine wameamini; ila siku moja karibuni, tabia ya Mungu itafutwa madoa machafu.

Jitahidi usiwe na mwelekeo wa kufanya kazi ili ucheze. Wanaume wengi wanaona kwamba kazi ni njia ya kupata pesa ya kununua vitu vya kujifurahisha wachezee siku wasizo kazini. Wanaume wana michezo ( adult toys) ghali kama vile magari ghali, pikipiki ghali, boti na vingineyo. Kumbuka kwamba kufanya kazi ili kutafuta riziki ni muhimu; ila kuna kazi nyingine pia za kusaidia watu kama wajane, maskini, yatima. Hii pia ni muhimu, kuleta kupona kwa wengine. Tumia karama na ustadi wako kufanya dunia iwe mahali bora.

Ili upate mahitaji kwa hali bora, wazazi wako wanafanya kazi. Mwana mwema hatataka kuchukua kazi au mali ya wazazi wake na kutumia kwa anasa zake. Unaporithi mali, uwe mwangalifu ili usaidie wengine wa kizazi kinachofuata. Tumeokolewa kwa neema na si kwa matendo yetu, hivyo tufikirie wengine na kizazi kingine.

Je, mwana anaogopa giza, mbwa, milima mirefu, au buibui? Kuondoa woga ni sehemu ya kukua na kuwa mwanamume. Inawezekana usiondoe woga wote, bali utanawiri na kushinda mazingira yako, japokuwa una woga fulani.

Musa alikuwa na woga huo, Kutoka 3-4. Yoshua aliambiwa, 'Uwe hodari na moyo wa ushujaa, usiogope wala usifadhaike, kwa kuwa BWANA, Mungu wako, Yu pamoja nawe kila uendapo.' Mtu anashinda woga wake kwa kujua kwamba Mwenyezi Yupo, na kwamba ana uwezo. Mwenyezi anajua unachohitaji, na atakupa ujasiri na kujiamini bali si kiburi. Ushindi unakuwa na utamu endapo umeushughulikia, 'Nawaandikia nyinyi vijana kwa vile mna nguvu na mmeshinda mwovu.'

Kila mwanamume anapata woga wakati fulani, hauwezi kushinda endapo hauna maadui wa kupigana nao. Kila mwanamume ana changamoto. Cha muhimu ni kushinda mapambano madogo unayokuwa nayo ya kila siku, mapambano yaliyo ndani ya moyo wako. Kuna siku hutataka kufanya kazi, bali itabidi ufanye. Ushindi unapatikana, hasa unapochukulia hasira, ulafi, tamaa za moyo wako kama maadui zako.

Asilimia 90% ya woga tulio nao ni vitu ambavyo havitatokea. Iliyobaki 10%, utapambana nayo, na unaweza ukashindwa machache, ila ukiendelea kupambana kwa nguvu, utashinda.

Uchoyo uwe mwiko, na kama una shida hiyo, si lazima uwe hivyo maisha yako yote. Mvulana atakuwa kiongozi wa nyumba yake na hata taifa, na kupanga mipango ya kusaidia watu, endapo ni mchoyo au anayejifikiria mwenyewe, ataumiza wengi. Wengi wanaosaidia mahitaji ya

**watu ya taifa kwenye ustawi wa jamii ni wanaume, hivyo mvulana ajifunze kuukana uchoyo au ubinafsi.**

**Kina mama wanatoa kwa ukarimu chakula au vitu vichache vya nyumbani, ila wanaume wanashughulikia mipango mikubwa ya kusaidia jamii na hata nchi nzima, na wakati mwingine kukiwa na matukio ya majanga au maafa wanaokoa wengi. Twapaswa kufundisha vijana wetu kutokuwa na 'umimi.'**

**Kijana aombe na kuwa mwazi kwa Mwenyezi Mungu, 'mimi nina uchoyo, najifikiria kuliko mtu mwingine. Najua hupendi niwe hivi, naomba unifungue macho yangu, nione mahitaji ya wengine ili niweze kuwa msaada. Naomba niwe na tabia kama yako.'**

**Piga picha baba yako anavyosikia akija nyumbani, je waweza kumsaidia kufanya jambo fulani, na mama yako waweza kumpunguzia uchovu wake? Ukimtembelea mtu angalia yale unayoweza kusaidia, badala ya kukaa kwenye kona utazamwe. Tumia muda wako kwa huduma ni msaada kwako kuondoa woga na uchoyo wa kujifikiria mwenyewe. Usiwe na haya au aibu, maumivu, au huzuni zako; anza kusaidia wengine.**

**Kila kiongozi mwenye njozi lazima afikirie kuhudumia watu. Watu wachoyo wanakosa ujasiri. Watu jasiri hawangoji nafasi kubwa za kuwa mashujaa au kuokoa watu, bali nafasi ndogo ndogo zinazojitokeza kila siku. Hizo zakupa nafasi ya kuwa jasiri au mwoga.**

**Jifunze kupenda vitu vya aina fulani. Wavulana wengi wanalalamika; 'Sipendi mvua, sipendi kazi niliyopewa, sipendi jua kali, sipendi kuishi mji huu, sipendi hichi kijiji, sipendi, sipendi sipendi!'. Kama unataka kufurahia ukuu na mema wa Mungu, jifunze kuyapenda yale aliyokuwekea wazi kuyapenda. Una uchaguzi, wa kulalamika na kunung'unika kwa kunyatisha sura, au kuvipenda vile ulivyopewa. Ila huna haja ya kuweka sura mbaya siku nzima.**

**Mwanamume mmoja alisema utotoni alikuwa hapendi nyanya, ila alipooa, mke wake alimpikia na nyanya. Naye akasema 'Nyanya hizi zinafanya nini kwenye chakula changu?' Lakini mke wake hakubadilisha kitu; akaanza kuzipenda na hata leo anapenda nyanya na anazimiss zisipokuwepo. Lakini twasema usipende uovu au vitu visivyo na afya, ila kuna vitu vingi waweza kujifunza kuchukuliana navyo na ukakuta unavipenda.**

**Wengi wamependa uyoga, au parachichi (ovacado), japo walishindwa kula vyakula hivi, walipokuwa wadogo kwa kubadilisha nia zao (attitudes). Kukomaa, na kukua ni kupenda mambo mengi yale machungu na matamu pia. Usijikaze tu 'kula nyanya' ila jifunze kuzipenda. Mungu ana mema mengi katika milki yake, tusiishi tukiepusha pua zetu kwamba 'sipendi ladha yake.' kwa vile Mungu alituruhusu tule.**

**Ili kuwa mwanamume kila mvulana ajifunze kuchukuliana na maumivu. Ni sehemu ya maisha ya kupata hekima, nguvu na ustadi. Mtoto asiyejikana nafsi, anapiga mayowe kwa maumivu madogo; anafikiri furaha yake zaidi ya majukumu yake. Badala ya kufanya kazi shambani anafikiria jinsi jua lilivyo kali, au kuchoka kwake. Badala ya kumpisha kiti mama mzee, anafikiria raha au burudani yake. Akijikwaruza mkono**

**kidogo, anakataa kuosha vyombo. Maisha yana maumivu mengi zaidi ya mikwaruzo midogo. Uumbaji wote unalalamika na maumivu ya aina fulani yawe ya kiroho, kimwili au kiakili. Hata wengi wana maumivu kwa mtu kusema maneno yasiyo ya upole, siyo tu kwamba wewe ndiye unayelengwa! Hivyo usijionee huruma ukiumia, kwa sababu kila kiumbe kinapata maumivu. Mwanamume apaswa kujua jinsi ya kuchukuliana na maumivu, hawezi kujificha, yaani kuepuka. Bila maumivu mara nyingine hakuna matunda au maendeleo.**

**Maumivu ni ya wote, na mara nyingi ni ya muda mfupi. Ila mbinguni hakuna maumivu, yale yanayotuumiza leo, yaweza kuisha kesho, hivyo usikite kwenye maumivu yako. Maumivu pia yana mwisho wake, ingawa kuna wakati tunaona tunashindwa kustahimili. Maumivu hayako huru kutufanyia yatakavyo kwani Mwenyezi anamiliki na kujua mwisho wa uvumilivu wetu, hivyo anatupa tu yale tunayoweza kuyastahimili. Mungu anajua kila urefu na uzito wa kila umivu, na ametoa ruhusa lije kwetu; 1Wak 10:13. Kama kisa cha Ayubu kinavyosema, hakuruhusu Ayubu kufikia anaposhindwa kustahimili. Maumivu yana uzuri fulani, Mungu hawezi kutupa bila sababu. Na mara zingine tunastahilishwa kuteseka na Kristo.**

**Mtu wa karibu nasi, anapotuumiza mioyo yetu kwa kutotuelewa au kwa mategemeo yetu kutotimizwa inatuumiza zaidi ya kawaida. Daudi alisema 'Kwa maana aliyetukana si wa mbali; kama ndivyo, ningevumilia. Aliyejitukuza juu yangu siye anichukiaye; kama ndivyo, angejificha asinione. Bali ni wewe, mtu mwenzangu, rafiki yangu niliyejuana nawe sana. Tulipeana shauri tamu; na kutembea nyumbani mwa Mungu pamoja na mkutano.'**

**Jinsi unavyojibu watu wanaokuudhi na kukwambia maneno ya kukuumiza, inaonyesha kama unakomaa kuwa mtu wa Mungu au unajifikiria wewe na maumivu yako tu. Mlilie Mungu ili akuliwaze, na usipige mayowe kwa muda mrefu kwa maumivu madogo, au kukasirika kama mambo hayakuendei unavyotaka.**

**Watu wengi wanapenda kuepuka maumivu ila wachache kati ya hawa wanafaa kwa ufalme wa Mungu. Ukiwa na maumivu au vidonda vya mwili, nenda hospitali ukashonwe, au kurudishwa mfupa sawa, ila usionyeshe kidonda chako kwa kila mtu.**

**Mwanamume lazima awe shujaa, asiyesihi kila mara huruma (pity) toka kwa kila mtu. Badala ya kuangalia kidonda chako kila wakati, angalia watu wa kuhudumia, ila utoe mawazo yako kutoka kwako na maumivu yako. Kwa maumivu ya moyo, usiwe kama mbwa anayelamba vidonda vyake siku nzima, ila 'ushinde wema kwa ubaya.' Hata Bwana 'Kwa ajili ya furaha iliyowekewa mbele yake, aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, Naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.'**

**Kuna wakati wa kutoa machozi, na kucheka. Siamini msemo kwamba 'mwanamume halii,' kwani hata Bwana Alilia; ila hakulia kwa huzuni Zake ila za watu wengine. Kulia kunapunguza maumivu ya moyo. Hivyo kuna wakati wa kujikaza, na kuna wakati wa kulia, na hiyo Bwana atawawezesha wana kutofautisha, ili wasiwe watu wa kulia lia ovyo, au kutolia na kupata**

shida za hisia.

Unawezaje kujitayarisha kuishi na mke vizuri sasa? Waweza kufikiri u mdogo bado, kufikiri hili na ukacheka, na ni kweli si wakati wa kuoa, ila waweza kujitayarisha wakati huu. Waweza kujitayarisha kimawazo sasa, ili baadaye uwe mwanamume wa furaha na kuwa na ndoa ya furaha. Siyo kwamba unaharakisha kuoa, ila ni bora uwe tayari hata kama hautaoa au ukipata wito wa kuwa towashi. Jifunze kazi ambazo wanaume wanasaidia dada zao, au mama zao; kama vile kubadilisha tairi, kukarabati nyumba, kuzibua choo, kuweka mbolea, kufuga nyuki, kuchunga mifugo, kung'oa visiki, kutumia nyundo na bisi bisi, kutengeneza zizi, kuchagua mbegu za kupanda, kuua panya au kupunguza matawi ya miti ya matunda.

Jinsi unavyowahudumia dada zako na mama yako sasa ndiyo darasa kubwa la ndoa. Wadogo zako wafurahi wana kaka mkubwa, wakupende, nawe uwapende pia. Jinsi ya kujenga mahusiano bora na dada au mama yako ndiyo jinsi ya kujenga mahusiano bora na mke wako pia. Usiwe jeuri, hata dada zako wakakuogopa na kutokwambia yaliyo moyoni mwao. Uwe na upole, ili wakuamini, na wakikuambia shida zao, chukua hiyo changamoto ya kuwatatulia bila kutangaza tangaza au kujisifu.

Je, wanapenda nini, au hawapendi nini? Je, unajua njozi zao na woga au mashaka waliyonayo? Je, wana mategemeo au matumaini gani ya leo au kesho? Ukiwa jeuri na mkatili, watakuficha. Kama dada yako alitaka kupata chombo cha muziki ajifunze, chukua changamoto hii na kumsaidia akipate.Dada yako ndiyo darasa la kukufundisha jinsi ya kutafuta riziki ya familia yako siku za mbele.

Ujasiri wa Daudi kumshinda Goliathi, haukuja siku hiyo hiyo; bali alianza kumpiga simba na dubu kwanza, ndipo akatoa woga na kuliendea jitu la kifilisti. Wahudumie madada na mama zako. Usiwe unawakejeli, kuwadhililisha, au kushindana nao kwamba wewe ndiye kijana au mwenye nguvu. Uwe timu moja nao, ikiwa chakula acha wao wapate sehemu kubwa nawe uchukue ndogo. Wape nafasi nzuri ya kukaa.

Je, umefikiria kuwaambia dada zako au nduguzo wadogo msome pamoja nao Neno la Mungu? Je, unaomba nao? Wasifu wakifanya mema, na wakifanya mabaya wasamehe, wasaidie wafanye vyema na kufunika makosa yao. Una nafasi ya kuwafanya wawe warembo nje na ndani ya moyo pia. Siku moja watasema, 'Kaka yangu alinipa nafasi ya kufikia njozi zangu, nampenda na kumheshimu.'

Mdogo, dada au mama yako akiwa wa kujifikiria na mchoyo msaidie. Mwombe Mungu akusaidie, na kazi yako itakuwa ni kurudisha mahusiano mema. Nawe pia uwe mfano kwa wadogo zako, dada na mama. Bwana amefanya mamilioni wasiompenda wampende, nawe fanya vile. Mvulana aliyekomaa haangalii nani anampenda na nani hampendi, bali anaangalia kufanya vyema bila kujali watu wanavyomtendea. Usifikirie wadogo zako, dada au mama hawataki uwasaidie na kuwapenda. Mara nyingi watabadilika. Wasichana wana kigeugeu wakati mwingine; ila wewe tafuta njia za kuwapendeza dada zako, mwulize hata mama yako, atakusaidia. Ni kazi ya mvulana na mwanamume kuwapendeza dada zake na hatimaye, mke wake.

**Unapochagua mke, mpe Mungu nafasi ya kukuchagulia, omba na ungoje wakati atakaokuchagulia. Mtu anachagua anayoona nje, ila BWANA anajua moyo. Angalia kama anapenda mambo ya kiroho. Epuka michezo rafu unayocheza na wanaume. Iwe mwiko kudansi na wasichana, maana inaamsha tamaa mbovu. Mashule mengi ya bweni yanaweka dansi na yamewaingiza vijana kwenye tamaa na dhambi. Kila siku tuna mapambano vichwani mwetu, na falme ya shetani. Vaa mavazi ya vita ya waefeso 6, usijianike kwenye majaribu. Epuka mahusiano yoyote ya ng'ono yaliyo ya dhambi, yapo mengi kwenye mitandao.**

**Dansi ni chombo cha shetani mwenyewe. Mwulize mwanamume yoyote kama atakubali mtu acheze dansi na mke wake wakikumbatiana, atakwambia la! Zama zile za ukoloni, watu walikatazwa kucheza ngoma za kienyeji eti ni za kishenzi, cha ajabu ni kwamba ngoma hizi watu walicheza mbali na mwingine, mwanaume na msichana hawakuwa karibu. Siku hizi dhambi zafanyika kwa wazi, za kukumbatia msichana asiye mke, kwa karibu yaani pungufu ya sentimenta moja.**

**Wengi wanafundishwa mambo ya kuvaa kondomu, ila kwa mtu anayemweheshimu Mungu. Ngono ni ya ndani ya ndoa tu, nje ya hapo ni dhambi au uasi wa sheria za Mungu . Hata hivyo kondomu haifuti dhambi, haindoi dhamira kushitaki, haizuii mimba au ukimwi kikamilifu au kutoa huzuni.**

**Mtoto wa kiume daima ajue kwamba ni Mungu pekee Ndiye msaada wa kuepuka dhambi za ngono. Wanaume wengi hasa katika ulimwengu wa leo wa ponografia (umalaya wa picha) wameangushwa au kuingia dhambini kwa mambo matatu yaani wanawake, pesa na kiburi cha mamlaka (power). Kama mvulana au mwanamume anajiona yeye hawezi kuanguka mtego huo, basi lazima atakuwa na nguvu kumpita Samsoni, Hekima za kumpita Sulemani na kumpenda Mungu hata kumpita Daudi.**

**'Apataye mke apata kitu chema na kupata ijara toka kwa BWANA.' Mvulana atofautishe kati ya mwanamke mgeni wa Mithali 7; yaani malaya na mwanamke bora wa Mithali 31. Je, ana tabia kamili za msichana bora? Je, anajua tendo la ndoa katika Neno la Mungu lina sehemu gani? Mfundishe mabadiliko ya mwili kama vile kubalehe, na endelea kuzungumza naye katika kila hatua.**

**Wazazi wengi wazungumza na watoto wakiwa na miaka kumi na mitatu na kuachia pale; kisha wanashtuka mambo yakiharibika wakiwa na miaka kumi na saba! Kumbe walitoa somo moja tu la ngono na kuacha! Majaribu ya ngono yanafikia wengi na punyeto; mtoto afundishwe kuepuka haya kila mara. Watenge watoto wako wasilale na watu wengine, na mambo ya sherehe za usiku (pajama party au sleep over) yawe mwiko.**

**Mvulana kujiweka safi kwa maneno, mawazo na mwili mpaka aoe. Je, ana mpango wa kumwendea baba wa msichana kabla ya kufungua ndoa na si kukaa pamoja bila mipango ya ndoa? (come we stay). Je, yupo tayari kukwambia anapotaka kuoa? Je, yupo tayari kukaa msela endapo Mungu amemwita kuwa towashi, na kutoishi maisha ya ndumila kuwili?**

**Biblia si kitabu cha ushauri bora au maoni bora tu, bali mawazo ya Mungu Mwenyewe, yenye mamlaka ya mwisho mbinguni na duniani.**

**Neno la Bwana latueleza jinsi ya kuchukuliana na kumpendeza kila mtu unayekutana naye, awe rafiki, dada, kaka, wazazi, mwajiri, wasichana, wazee, maadui au watoto. Inawapa watu tahadhari na mitego, inakueleza jinsi ya kufanya kazi, kuwekeza pesa, jinsi ya kula, cha kula, na hata wakati wa kulala. Ina kanuni za kila nyanja ya maisha yako. Inatupa kina cha kujua Mungu anavyofanya kazi na jinsi ya kusikia sauti Yake. Inafanya tujue maisha, mambo ya asili na hata ya sayari nyingine. Inatueleza kuanzia Mwanzo mpaka ufunuo jinsi ya kumpokea BWANA aliyejitoa kwa ajili yetu kwa kutupa uzima wa milele.**

**Wewe siyo mnyama kama elimu ya uibukaji inavyopoteza, umeumbwa kwa makusudi maalumu. Kila mvulana ajiulize yupo hapa kwa ajili gani, ametoka wapi, na nini kitatokea akifa. Neno la Mungu laeleza kwa nini kuna maumivu haya yote. Hakuna kitabu chochote kitakueleza yote haya. Saa moja kwenye kitabu kingine kamwe haitalingana na saa moja kwenye Neno lake.**

**Hakuna kitabu cha kusisimua kama hiki, na kinachobadilisha maisha ya mtu. Hesabu au kemia haiwezi kubadilisha maisha yako kama kitabu hiki. Ila Biblia si kitabu cha kupata habari bali kubadilisha maisha (not for information but transformation). Ukifuata ushauri wako, mambo yatakuwa halisi na utabadilishwa. Usipoteze muda kusoma hadithi za nadharia (novel) au fictions ambazo zinafanya usipende kusoma Neno la Mungu. Hadithi za kufikirika zafanya Biblia isiwe na ladha.**

**Akili zako zitapanuka, ukisoma Neno hili na hata utakuwa na uwezo mkubwa darasani. Soma na elezea marafiki, ulichopata kwenye sura hiyo. Wakati mwingine unyamaze kwa utulivu na kuangalia Utukufu wake. Kariri mafungu yake mengi, imba nyimbo. Marko 1:35 inasema, 'Alitoka kwa faragha aende kusali;' nawe, amka na ukasali.**

**Sikiliza mausia ya wazee, hautakuwa kama rika lako bali utakuwa na hekima ya kupita umri wako. Mashauri haya ya wazee yanaweza kuonekana yamepitwa na wakati, ila utakuwa unatafuna mambo na kucheua kwa hekima ambayo watoto wa umri wako hawana. Twaona Sulemani alipokufa kijana wake Rehoboamu aliomba ushauri kwa vijana wakampotosha, naye akapoteza ufalme wake.**

**Wazee wenye hekima hawazungumzi mawazo yao kwa haraka, wanapima mambo kwanza. Wanajua maisha ya mvulana au mtoto yatakuwaje, hata kama hawakwenda shule; kwani miaka ya uzoefu waliyonayo inawasaidia. Wengi wamepinga ushauri wao, na hii imewafanya wanyamaze, wakiogopa kujichumia uadui na vijana. Hivyo ni jukumu la wavulana na vijana kukaa na wazee na kuwauliza maswali ya taaluma nzuri ya kusomea au ustadi gani ni wa muhimu kupata, au uwekezaji gani bora, n.k.**

**Mpepeleze mzee kwa maswali kama haya: Je, mtu afanye yapi kuwa na mahusiano mazuri? Je, mambo gani yanaharibu mahusiano? Je, jamii imebadilika kwa namna gani leo? Je, imebadilika kwa mazuri au mabaya gani? Ni makosa yapi uliyoyafanya mambo yakaharibika? Ni sehemu gani ya maisha yako mambo yalikuendea vizuri sana? Nini waweza kunielemisha kuhusu ndoa na kuwa na watoto? Ukiwa mwajiri, ni mtu gani**

utamchukua kwenye kampuni yako? Ukiwa mdogo wakumbuka ushauri aliokupa baba yako? Je, uliufuata? Je, ni nini kilicho muhimu sasa kwenye maisha yako? Je, upo tayari kufa wakati wowote? Kama ndiyo! kwanini? Kama la! Kwanini?

Kuna wakati wa kuua na wakati wa kuponya (Mhubiri 3), na hiyo ni changamoto ya kukua au kuwa mwanamume. Watu wengi wanachanganyikiwa na kuua wakati wasipopaswa na kutoua wanapopaswa. Je, mvulana atajuaje? Mwanamume au mvulana si mnyama mwingine kwenye himaya ya Mungu. Alipewa mamlaka na milki. Anapaswa kuheshimu viumbe na kuwa wakili bora, si kuua viumbe au kukata miti bila sababu, eti alimradi iko kwenye milki yake. Anapaswa kuvitumia hivi vitu kwa mahitaji yake, ila si kwa ufujaji, akikata miti apande miti. Asiwe mkatili, ajue kuhifadhi, pia ni kitu gani atakachokihifadhi. Mfano, panya wako katika nyumba wanakula mahindi yako, Je, uwaue? Siafu walio porini uwaue? Je, paka anayekatisha barabara umuue? Ukiwa unaishi karibu na mbuga ya wanyama na una njaa, je, uue swala bila kibali? Usipuuzie kazi ambayo Mungu alikupatia, ya kuhifadhi na kujali viumbe. Hata wanyama wanajua ni nani anamcha Mwenyezi Mungu kutokana na huruma na utunzaji wanyama anaofanya huyo mtu. Je, mifugo yako inapewa malisho au chakula na kushiba? Au unafuga mbwa bila kumpa chakula mpaka mbavu zake zinaonekana? Kumbuka Nuhu aliambiwa aweke wanyama kwenye safina, Mungu aliweza kuwaumba wengine, ila aliwapenda wale wanyama. Biblia yasema Mungu akamkumbuka Nuhu na wanyama.

Ili mtu akidhi mahitaji ya familia yake kiriziki anahitaji kuua mara nyingine, ila asiue viumbe vya Mungu kwa ajili ya hasira au futuhi bali kwa riziki au ulinzi. Wakati vita vimetokea, tunajua wazi kwamba watu wengi wanaompenda Mwenyezi Mungu wamepigana vita vya kuleta uhuru na kulinda nchi zetu au jumuiya. Wengine kutokana na dhamira na sehemu Mungu amewapa kufanya, wamekataa kuua kwenye vita na kushughulikia majeruhi wa vita na hiyo ni sawa kutokana na mtu na kuelewa mambo fulani (non-combatant). Ila wanaume wote lazima wajue jinsi ya kulinda familia zao na kujua kuleta riziki.

Mwanadamu ana jukumu la kutunza hifadhi za karibu na kwake na kutokuwa mharibifu. Wavulana wengine wamepiga ndege kwa manati na kucheka tu bila sababu yoyote ya maana. Mwanamume anahitaji kutunza vile Mungu amemkabidhi, yakiwemo mazingira. Tunaishi wakati ambao watu wanaua hata watoto wao wenyewe kwa kutoa mimba au njia zingine. Watu wako tayari kuua watoto wao ila wanaogopa kuua mende kwenye makabati yao. Lazima tujue thamani ya binadamu, na wakati huo huo kuwa na ujasiri wa kuua vitu kama mende au panya.

Ibada ya nyumbani ni muhimu. Usikunje ndita wakati wa maombi au ibada. Waisraeli walichukua muda mwingi wa ibada, na kutoa kafara, ila walikuwa na kujifikiria na uchoyo. Kila siku ni siku ya ibada, pia kwa jinsi tunavyoishi tunaabudu. Maana twaweza kuwa waimbaji wazuri ila maisha yetu yana harufu mbaya. Twahitaji mioyo yetu kubadilika, ili tusiwe na vichwa vilivyojaa Neno la Mungu bali mioyo iliyojaa dhambi.

**Kama unataka kuwa mwanamume wa kweli ambaye Mungu atamtumia, jifunze kumwabudu Mungu jinsi anavyotaka kuabudiwa. Mwabudu kila siku katika uzuri na Utakatifu wake. Mahusiano na mawasiliano ni muhimu. Jifunze kuandika barua za kutia watu moyo. Jifunze kuandika barua rahisi, na unapoendelea kuandika utakuwa na ustadi huo, na utakuwa na barua nzuri. Wengi wanapata barua za kulalamikiwa, na watakapoona barua ya kushukuriwa, watashangaa na kupata ujasiri na watatunza barua yako milele.**

**Ninapoishi, watu wengi wanaogopa kupokea zawadi kwa ajili ya kujisikia wana deni, kiburi au hawataki kuwa kwenye 'mgawo wa ustawi wa jamii.' Wengine wanaogopa kuandika barua za kushukuru. Kutoa na kupokea zawadi kunajenga mahusiano mazuri. Ukiacha kupokea zawadi watu watafikiri kwamba wewe unaona vitu vyako ndiyo vya maana, au hutaki kutoa vyako na hivyo, unawafungia mlango. Kutoa ni mbaraka kuliko kupokea hivyo usifanye watu wengine wapoteze baraka zao kwa kutopokea vyao, wakikupa kitu kwa nia nzuri.**

**Kwa watoto wetu, tunawapa mazoezi ya kutoa tukipokea pia. Ila andika barua ya kuwashukuru na ukilenga kile unachoshukuru; mfano: 'Asante kwa hela, zimenisaidia sana msimu huu kwa kilimo cha matango.' Wengi waandika barua kuomba vitu wakiwa wanafunzi shuleni (boarding), bali wakiwa watu wazima na hawahitaji kitu, hawaandiki ng'o; hili ni kosa. Mawasiliano si kwa kupata vitu bali huduma ya upendo.**

**Twajitayarishaje kuwa baba bora tukiwa vijana wadogo? Jibu: Kwa kufanya vile ambavyo tungetaka watoto wetu wawe! Usifikiri jinsi utakavyowalea watoto wako, bali fikiri vile Mungu anataka uwe kama Yeye. Watoto wako wakiwa rika lako, Je, wataka wawe wa tabia gani? Maana watoto wako watataka kuwa kama wewe. Je, wewe ni mwaminifu? Je, ni mtenda kazi mwema? Je, wapenda kunung'unika kila mara? Fahamu kwamba watafuata mfano wako.**

**Mungu ana huruma, japokuwa umeharibu mambo. Maana hatupi tunayostahili (exceptions). Si tabia zako zote mbovu zitaelekea kwa watoto wako bali 'tunda halianguki mbali na mti.' Watoto utakaozaa watafanana na wewe. Mvulana wako akiwa na miaka kumi na miwili atakuwa kama wewe ulivyokuwa miaka na miaka kumi na miwili. Kama u mvulana mwenye shukrani, na mwenye bidii naye atakuwa vile vile, ila kama u mvivu atarithi tabia hiyo mbovu. Ukiwa na bidii ya mazoezi ya chombo cha muziki, naye atakua vile. Somo lolote utakalofanyia bidii naye pia atalifanyia, unachofurahia nao watafurahia. Mfano wako utawafundisha mno.**

**Tabia ya leo itakufanya uwe mwanamume wa kesho, na hiyo itaathiri watoto wako. Waweza kufikiri mimi ni mtoto tu, nitashughulikia hili au lile nikiwa mtu mzima. Utashangaa siku zimefika, na u mtu mzima na kufanya tu yale uliyoyafanya ukiwa mtoto! Hivyo anza leo kubadilisha mwenendo, una nafasi ndogo ya kubadilisha mwenendo kesho.**

**Uwe na njozi ya kufanya vitu kama mwanamume, na njozi hizi za hekima na maarifa zitakusaidia uwe na mahusiano mazuri na utajiri wa kikweli (true wealth). Kila siku hujenga matofali ya tabia ambayo inakuwa ngumu**

**kama simenti, ikiwa mbaya ni kazi kuiondoa kizazi kinachokuja.**

**Tabia njema ni kama kuweka akiba kwenye akaunti ya watoto wako. Ukielewa somo, utaepuka mashimo mengi, wavulana waweza kubadilisha mambo kirahisi kuliko wanaume wazee. Angalia maisha yako kwa uaminifu na uyakague vizuri, waulize marafiki au wazazi wako udhaifu wako na uzuri wako. Mwombe Mwenyezi akufanye wewe uwe mwanamume ambaye unafaa, kisha uanze kubadilisha mwenendo leo.**

**Je, mwana aweza kuongoza maombi na kusoma Neno la Mungu na kuneemeka? Je, aweza kugawa mamlaka hata kwa ndugu zake wafanye? Lazima kuwe na ratiba ya kufanya kazi kwa watoto wote nyumbani.**

**Kusaidia vilema na kutowacheka au kuwakejeli ni muhimu. Ninapoishi, mtu mmoja wa Afrika mashariki pamoja na mkewe, walikuwa wakicheka vilema wenye vichwa vikubwa na utindio wa ubongo, walipofanyia kazi. Walipofunga ndoa na kupata mtoto wa kwanza alikuwa na kilema kigumu cha kukosa njia yote ya mkojo, Ilibidi waishi hospitalini. Watu walisema, 'sasa hawana haja ya kucheka mbali, wana cha kucheka karibu, nyumbani mwao!' Walinyenyekea na kuwa watu wanaoelewa shida za watu. Ni kweli mara zingine tunapata shida ya ulema hata kama hatukucheka, maana mapenzi na utukufu wa Mungu hatujui, lakini tunapocheka shida za watu dhamira hutushitaki.** www.truthforyourfamily.org **by Joel Beeke.**

**Ukitaka kuwa mtu mcheshi mwenye bidii, watoto wako watakuwa vile pia. Watapenda kazi kama baba na kuwa wacheshi. Utasema, inakuwaje nami ni mvulana hivyo hawanioni sasa? Mpango wa Mungu wa kuishi, kwamba mti mzuri unatoa matunda mema, si kwa kubahatisha tu, bali ni kanuni ya mbinguni.**

**Je, mtoto anajua maana ya uovu ni nini? Anajua amri kumi kwamba ndiyo kipimo cha haki? Je, anajua rehema za Mungu na kutendea watu kwa haki au ana ubaguzi? Maana Mungu anataka tuenende kwa haki, rehema na unyenyekevu. Je, aweza kuwakanya ndugu zake? Je, anapata hasira na kuwakasirikia ndugu zake? Je, hapendi kusahihishwa? Apaswa kujua kusimamia nyumba yake vizuri? Watoto wapewe kazi kutokana na umri, mfano kusafisha gari, kukata majani, kulima shamba, n.k.**

**Kukana nafsi ni muhimu kwani bustani ya Edeni ilipotea kwa kutotawala tamaa ya chakula, na ulafi. Mtoto afundishwe kuepuka hali hii. Kulinda moyo wake na mafikira kwa kutoangalia vya vipindi vya kuangusha kwenye Televisheni, simu na kompyuta zenye programu mbovu.**

**Aepuke kuingia kwenye madeni. Zungumzieni mambo ya madeni na jinsi ya kuepuka. Hasa siku hizi za madeni ya kadi- credit cards. Alipe ikiwezekana na ajifunze kutoa sadaka na zaka. Asiwe mtu mwenye hasira, 'Asiyetawala roho yake ni mfano wa mji uliobomolewa, usio na kuta;' Mithali 25:28. Hata mtoto mdogo afundishwe kungoja bila kuwa na hasira, anapocheza na wengine.**

**Hasira zisizoweza kumilikiwa zinaweza kuumiza mke au watoto au mtoto wa kiume mwenyewe. Akiwa anashindwa kutawala nafsi, na kuwa na harara mfundishe 'kutojisumbua kwa neno lolote, bali katika kusali na kuomba akishukuru aweke haja zake kwa Mungu, na amani ipitayo akili**

**itamhifadhi kwa moyo na nia.' Akiendelea kutumia kichujio cha mambo yote kwa yale yaliyo ya kweli, ya haki, safi, yenye kupendeza, yaliyo na staha, mema, na sifa nzuri, na kutafakari hayo.**

**Ajifunze jinsi ya kuhudumia familia, na kuwa na adabu njema (manners), maana hizi haziji zenyewe bila kuzifanyia mazoezi. Ajifunze kusema samahani, pole , asante, tafadhali, nisamehe, naomba. Ajifunze kutonyanyasa watu walio chini yake, maana watoto wengi walionyanyaswa na wazazi wao huendeleza tabia hiyo, ila aende mbele za Mungu, kuzikanusha nguvu hizo za giza, au laana hiyo ikatike katika kizazi chake, ili isiendelee kizazi cha tatu na cha nne.**

**Je, ana muda mwingi wa kupoteza akikaa kwenye media au mtandao. Je, anajifunza tabia za kuwa mtu wa bidii? Je, waweza kumtegemea akufanyie kazi fulani bila kupeleka mawazo yake kwenye vyombo vya teknolojia? Je, marafiki zake wa karibu wanampenda Mungu au apenda kujiegesha na watu waovu kama Delila? Je, anajua jinsi ya kuwa na urafiki wa kawaida na wasichana bila kujiingiza kwenye urafiki mbaya? Je, ni tabia gani za kuepuka kwa marafiki?**

**Je, anatoa udhuru wa kuhudhuria ibada? Je, kila saa anatoka kunywa maji au kwenda chooni wakati wa ibada? Je, anamtegemea Mungu au ananung'unika mambo yasipoenda vizuri? Je, anaweza kumaliza kazi uliyompa kama vile Nuhu au Nehemia? Je anaweza kutimiza ahadi zake kama vile Elkana na mke wake? Au mawazo yake yanatawanyika huku na kule? Je, vitu vyake aviacha kila mahali? Hata akivua nguo suruali yake inasimama kwenye sakafu pale pale alipovulia?**

**Mara zingine wazazi wanahusika na kuhudumia watu, na mtoto anapata amakini ambayo wazazi hawajui. Hili nilijifunza kwa mhubiri Billy Graham, alipokuwa mashuhuri sana, watoto wake walikaa karibu na lango (gate) la nyumba na kabla wale watu kumtembelea mhubiri, wale watoto waliwaomba washiriki pesa au vitu. Wageni waliona aibu kwaajili ya baba yao wakawapa hawa watoto vile vitu, bila ya kuripoti kwake. Tabia hii alikuwa nayo Gehazi mtumishi wa Elisha! Aliomba nguo mbili na visenti na kupaka matope kazi kubwa ya mtumishi. Mhubiri huyu alikuja kugundua baadaye, kama wewe mzazi u mashuhuri au wahusika na mambo fulani ambayo watu wengi wakujia, angalia watoto jinsi wanavyohusika na watu, ili uwaepushe na uovu wa namna fulani.**

**Je, anaweza kuwa mkarimu kama Ibrahimu kukaribisha watu asiowajua na kupata mibaraka? Soma kuhusu ukarimu na kukaribisha wageni. Je, anajua ukarimu kwa familia yake pia? Je anaogopa kupokea simu, kujibu barua au kufungulia wageni milango? 'tazama nabisha mlangoni. Yawezekana Yesu akabisha mlango. Siku hizi pengine hatupati wageni nyumbani ila hata simu zetu mara zingine ni watu wanaohitaji ushauri au huduma kutoka kwetu. Nimejifunza mara nyingi pia ni watu ambao wananibariki mimi, na si mimi nawabariki, kama vile Abrahamu, mgeni yule alimbariki, na si Abrahamu alimbariki yule mgeni! Mwana ajifunze kuwa mhudumu, na si kuepuka wageni**

**Basi mtoto wa kiume asiyejua kutafuta riziki, ni mwovu zaidi ya yule asiye muumini. Japokuwa wanawake wanajitafutia riziki wenyewe siku**

**hizi, hili ni jukumu la kwanza la mwanamume. Hii inataka mwanamume asiwe mbinafsi, na wazazi tuwasaidie watoto wetu wa kiume waweze kuwa watafutaji kwa njia halali. Wasaidie wadogo zao, babu na bibi na pia miradi ya familia. Zungumzeni bajeti ya familia, na jinsi wanavyoweza kutafuta vibarua vidogo vidogo.**

**Je, aweza kujitafutia mahari yake mwenyewe? Je, anajua jukumu la kutunza wazazi waliozeeka? Je, anasaidia kazi za nyumbani kwa uaminifu? Je, ana ukarimu wa kusaidia wenye mahitaji na kumwonyesha jinsi ya kufanya? Ajifunze kuwa msikilizaji mzuri, na kutoingilia mazungumzo ya watu wengine**

**Je, anakumbuka kuwaombea wengine au huwa anajifikiria na kuleta shida zake tu mbele za Mungu? (maombezi) Je, anajua kuungama dhambi akikosa? Je, anajua kusimulia kisa cha wokovu kwa dakika chache, akielezea mafungu yake?**

**Je, anataka kuoa binti wa namna gani? Je, anawaheshimu wasichana kama ni wake za watu wa siku za usoni na hivyo anawakinga na uovu, na uchafu ili wawe mabikira kwa waume zao baadaye?**

**Mara nyingi tumejaribu tunavyoweza, hapo tunamwachia Mungu ndiye MWEZA. Hatuwezi kujua kwa nini jambo fulani limetendeka kwetu, ila matukio mengi tunaweza kujua mwishowe yana mshahara gani.**

**Mvulana atakayeishi kutokana na hukumu na sheria za Mungu atavuna matunda ya watoto wanaompenda Mungu siku za usoni. Mithali 22:6. Hivyo unapojaribiwa kufanya uovu au upumbavu fulani, kama kuvunja sheria, fikiria maamuzi yako, na kwamba yatajirudia kizazi kijacho, hata cha tatu na cha nne. Hivyo ghairi ukanuie kuishi kwa msingi bora wa vizazi vijavyo. Utaishi bila majuto, na itakuwa ngome kwa watoto na wajukuu wako, Mungu atakapokujalia. Tukumbuke Mungu ni mvumilivu, mwingi wa rehema, na anasamehe uovu.**

**Je, mwana anapasa kuwa na uhusiano gani na kileo? Jibu ni 'Asijaribu kuweka mdomoni, hata tone la pombe;, asivae hata tshirts zenye matangazo ya pombe au kileo au kusikiliza matangazo ya biashara ya namna hiyo. Asiende mahali ambapo kileo kinapouzwa au kumcheka mtu aliyelewa maana dhambi ni kitu cha huzuni. Kataa kutoa sababu kwamba ni lazima unywe, hata kama huna mpango wa kunywa, jua ni jaribu linaloweza kukujia, kwani wengi hawakufikiri wataingia katika ulevi. Waambie marafiki zako kwa upendo kwamba hutakunywa na sababu unamheshimu Mwenyezi Mungu. Mithali 23:32 yasema, 'Ukae mbali na kilevi chochote kama unavyoweza kukaa mbali na nyoka.'. 40% ya wanywaji hawawezi kuacha (alcoholic). Je, Ukiwa na mbwa anayeuma watu 2 kati ya tano wanaokuja kwako utaendelea kumfuga?**

**Mwana ajue kwa nini anapata adhabu au masahihisho ya tabia yake ili aongozwe katika njia njema ya hekima. Mwana anayependa wazazi wake atawashukuru pale wanapomsaidia. Ajiepushe kuharibiwa na misukumo ya rika ndiyo iliyomponza Samsoni. Kumpenda Mungu na kutembea katika njia zake na kumtumikia kwa mioyo, akili, nguvu na roho zetu ndiyo hekima. Maneno yake yawe yametiwa munyu ili ajue kujibu watu maana maneno yanaonyesha tabia na kile kimeujaza moyo wake. Usafi wa moyo,**

**maneno, na matendo (purity) ni muhimu.**

**Kukuza mtoto wa kike awe mwanamke wa mithali 31-Mafunzo kwa mama na binti.**

Daudi, mwandishi wa Zaburi, azungumza maneno ya baraka kwenye Zaburi 144:11-15. "Wana wetu wawe kama miche waliokua ujanani, na binti zetu kama nguzo pembeni zilizonakshiwa na kupamba hekalu…".

Bila shaka kukuza mabinti zetu mpaka utu uzima wakiwa wanampendeza Mungu ni baraka kubwa. Wazazi wengi kwa kuwa na shughuli nyingi, wanajaribiwa kuacha watoto wajikuze wenyewe. Mungu hakutupa watoto tuwatelekeze (neglect). Uzazi ni jukumu zito, kuliko wengi tunavyofikiri. Kina mama hatuwezi kuacha watoto wetu, hata wa sekondari, wakiwa ndani ya nyumba peke yao, na sisi tuko busy, au tunasafiri kila wakati.

Wengine twafanya kazi za shift, wengine twajitembeza hapa na pale, na tunaacha watoto peke yao; hili ni kosa. Mawazo ya mtoto yanatembea huku na kule wakati mwingi. Aweza kwenda kwa majirani, au kuangalia mambo yasiyofaa n.k. Maisha ya Dina mtoto wa Yakobo ni mfano. Wanaweza kuanza kufanya mabaya, ila usiwe wewe ndiye uliyetoa nyufa. Wengine wamepeleka watoto wadogo magharibi wakawaacha huko wenyewe, bila wao kuwepo. Wengi walishindwa kumaliza shule, bali la kuhuzunisha zaidi, ni kwamba wengi waliacha imani. Waliingia kwenye ndoa za ajabu ili kupata vibali vya kazi, na kupigana na wenyeji wa nchi hizo, na wengine wakawa hoi, kwa michoko. Sulemani asema mtoto ana ujinga wa namna fulani ulioshikama na moyo.

Masomo ya chuoni au kwenda Magharibi yamekuwa kama miungu fulani siku hizi za mwisho. Maisha ya kumcha Mungu ni mpando. Usiache mtoto wako kwa mtu akuangalilie kama siyo dharura, kwani utamlaumu huyo mtu. Watoto wana mambo mengi na hufanya majaribio kuona itakuwaje; hata kama ni mtu mwema umempa hiyo shughuli. Hata hivyo ana uchungu gani na mtoto wako zaidi ya wewe mzazi?

Tulikutana na msichana mkubwa wa sekondari, aliyelelewa mbali na wazazi wake, ambaye hakusalimia watu, hakushukuru watu walipomtendea mema, wala hakufungua mdomo wake aliposalimiwa au kuulizwa maswali ya kawaida. Tulidhani ni bubu au kiziwi, bali tuligundua ni tabia alivyokuzwa bila kufundishwa adabu, au kutofahamu, (ignorance). Wengine wakasema ni 'mtu wa haya'. Haya na kukosa adabu ni vitu tofauti.

Mabinti wetu wanahitaji mafunzo (training), kwani siku za usoni watakuwa walimu wa watoto wao na watahitaji mawasiliano bora na waume zao na hata wakwe. Je, unaweza kumkanyaga mtu kwa bahati mbaya na kutotoa hata samahani? Hata hivyo yeyote anayetaka kuwa raia wa ufalme, lazima ajue kuwaambia watu habari njema! Je, atanyamaza kimya, eti anaona aibu ili aakienda sokoni anajua kubembeleza bei apate dili na nyanye zishuke bei ili apate manufaa?

Mithali 31 ina mengi ya kusema kuhusu mwanamke anavyopaswa kuwa. Nafikiri jambo hili linaanzia katika matunzo udogoni, na si ukubwani. Wengi wamesema mwanamke wa mithali 31 ni muunganiko wa wanawake wengi! Tunaona ana watu wa kumsaidia kazi zake, ila ni yeye anabidi kupangilia

mipango ya mambo ya kufanya. Kama wazazi na hasa kwa wanawake, tuna haja ya kujifunza zaidi kuhusu mwanamke wa Mithali 31 kwa undani. Maswali haya na majibu ni kwa mjadala na mabinti zetu. Tuendele kuwaongoza na kuwathathmini, nasi wenyewe tutazidi kukua katika safari ya kwenda mbinguni.

Mama Pam Foster wa doorpost.org amemzungumzia mwanamke huyu kwa undani. Tumechukua maswali yake, nawe utachukua nafasi kila siku kujadili na binti yako, na kumfundisha yanayohusu maswali haya ya Mithali hii 31. Ni vyema msome pamoja kitabu chote cha Mithali, Mhubiri, na Zaburi. Chukua muda kusoma Neno la Mungu lote kila jioni kwa miaka mitatu, mkisoma sura moja mojaya Biblia na kutafakari na kuwa na maswali mtajifunza mengi ya kulea tabia ya kufaa kwa mtoto. Hakuna kitabu bora kwa kukuza mtoto kama Neno la Mungu Mungu Ndiye msazi mkamilifu. Binadamu aliye mzazi ni mwenye dhambi anayejitahi kumkuza mwenye dhambi mwingine (A sinner raising another sinner)

Je, anaelewa kwamba uumbaji kwa siku sita na mapumziko ni mhimili kwenye mafundisho ya Neno la Mungu? Siku hizi nadharia za kuibuka (evolution) zimezuka na kufanya mabinti zetu wasijithamini, kwamba wameumbwa na Mungu! Siku za Mwanzo moja ni siku halisi za masaa 24 na si mamilioni ya siku.

Somo la kwanza kwa watoto wetu ni utii. Twarudia "Utii" ndiyo somo la kwanza!". Kutii maagizo ya Mungu na wazazi. Tunakumbushia tu kwamba maneno haya yalizungumzwa na mama yake Sulemani, akimwambia kijana wake jinsi ya kuona mwanamke bora! Kinyume cha mwanamke bora ni mwanamke wa Mithali 7, ambaye ni 'mwanamke mgeni au wa mitaani' (strange woman).

Lazima sisi wanawake tuwe watu wa kusali kwa kukesha na kuwa na mipango/magoli kamili ya kulea, na kuyaweka kwenye karatasi. Kama tunataka tuwe na mabinti wa mithali 31 lazima nasi waone mifano yetu . Hivyo tumwombe Mungu atupe nguvu, tufunge mikanda ili tusaidiane na mabinti zetu. Mabinti wajifunze utii, mipangilio, kujikana nafsi, ustadi, usafi, na kazi. Wote tungependa tuwe na mabinti waliokomaa kiroho, kiakili, kijamii, kiuchumi na kimwili pia.

Mwanamke huyu anazungumziwa kwa undani sana. Twaona anatayarisha chakula, anashona nguo zake na za familia, anafanya ujasiliamali, ananunua mashamba na kulima, ananunua nyumba, anapanda mizabibu, anasaidia wenye mahitaji. Ni mwanamke wakupendeka (admired).

Wanaume pia wangependa kuwa na dada, mama, binti au mke kama huyu. Hata kama mume ni mtu asiyeamini, aweza kubadilika kwa mwanamke kama huyu. Wanawake wana sehemu kubwa katika malezi, twaona Timotheo, mhubiri mkubwa alipata imani toka kwa bibi yake Lois, na kisha mama yake Yunisi. Tusichoke kutenda wema maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho.

Wanawake wengine wamekata tamaa kutokana na maisha magumu ya mateso, mwingine alisema "Nimekinywea kikombe." Ni kweli wengine wameangukia pagumu, hata hivyo tusichoke, tusipozimia roho, hata kama binadamu na wale wa familia yetu ya karibu wasitusifu, wasituthamini (appreciate) au kutupenda, wito wetu kwa neema za Mungu, ni kuishi maisha ya mwanamke wa Mithali 31. Na kusema nitakwenda ulimwenguni kote kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi.

Mambo haya ni ya kufanya na mabinti zetu wakikua. Pengine yapasa tuwe na vitu vichache ili tuwekeze kwa watoto wetu hazina mbinguni badala ya duniani. Tusifikiri masomo ya shule tu, bali hata ya nyumbani. Ni vyema kuwa

na mpangilio (ratiba) ya kusaidia watoto tabia na taaluma; maana hata hekima ya dunia tunayoikazania sana yaweza kuwa upumbavu kwa Mungu; 1 Kor 3:19. Waweza kuleta topic kwenye maombi, kuhoji watu, kutenda vitu (practical), kujadili, mafungu ya kukariri kutokana na topic, kuuliza maswali, kusoma vitabu vingine vihusuvyo tabia tunazozijadili na mwishowe kutathmini, ili wakue kiroho katika ile nyanja mnayotaka kuijenga.

"Upendeleo hudanganya, na uzuri ni ubatili, bali mwanamke amchaye Bwana ndiye atakayesifiwa. Mke mwema ni nani awezaye kumwona? Maana kima chake chapita kima cha marijani" (rubies); Mithali 31:10. Fungu hili linatuambia tuombee mabinti zetu kuwa na roho za unyenyekevu, na upole mbele ya Mungu, kuwa tayari kusikia na kulitii Neno lake.

Wape nafasi wamhoji bibi au mama mwenye mvuto wa kumpenda Mungu na kuomba ushauri Wake. Wape nafasi mabinti/binti zetu ya kuzungumza na baba, au wajomba zao na kuuliza ni sifa gani iliyowavutia kuoa yule waliyeoa. Je, katika Neno la Bwana wanawake kama hawa ni kina nani? Toa mifano ya visa vya wanawake kama Debora, Esta, Hulda, Elizabeti, mke wa Ayubu, Ruth, binti za Lutu, Tamari, Safira, Goma, Prisila, Abigaili, Yezebel, Bathsheba, Raheli, na Rebeka.

Soma Tito 2 na andika orodha ya mwanamke amchaye Mungu. Soma 1 Tim 5:3-10 inayofanya mjane athaminiwe na kusaidiwa. Jiulize maswali kuhusu binti yako kama anampenda Mungu, na kama wokovu wake ni muhimu kwake. Je, anapenda kusoma Biblia, au anafurahi akisomewa kama ni mdogo? Je, anaelewa Neno la Mungu? Je, anapenda kumtii Mungu? Je, ana mahusiano na Mungu? Je, akifanya makosa, anajutia dhambi na kuomba msamaha kwa Mungu na wale aliowakosea? Je, anapenda kuwa kama wasichana wa dunia kwa mavazi, michezo na mwelekeo? Je, ana udhaifu fulani wa tabia? Je, anafanya jambo gani kuondokana na udhaifu huo. Je, lile tunda la Roho la Wagalatia 5:22-23 linaonekana katika maisha yake? Je, wawezaje kumsaidia katika nyanja hizi za tunda? Je, anakua akiendana na Mithali 31 na Tito 2? Je, ana magoli ya kumtukuza Mungu na kuwa mhudumu kwa Mungu na familia yake, au anajipenda na kutafuta anasa zake za kujinufaisha tu?

"Moyo wa mume wake humwamini, wala hatakosa kupata mapato," fungu la 11. Mume wake anaona kwamba ni mke anayechukua majukumu yake kwa makini. Lazima tuwatayarishe mabinti zetu kwa hili, kwa kuwafundisha (train). Elimu ya binti yako ni muhimu, na inafanywa nyumbani. Ajue kazi za nyumbani, mpeleke kwa mwanamke ambaye ana bidii ya kufanya majukumu yake vizuri, amhoji kwa nini anafanya shughuli zake kwa uaminifu? Kwa nini awe mwaminifu katika kazi? Jadili naye mifano ya uaminifu kwenye Biblia toka udogoni kama vile Ibrahimu, Yusufu, Daniel, binti mtumwa wa Naamani, Delila, Mikali, mke wa Potifa, mke wa Hamani, Herodias, Hawa, au Tabitha. Umepita wakati wa jando na unyago, mabinti walifundishwa haya, leo hii mfundishe binti wewe na waumini wenzako. Usiseme 'shangazi' au wifi ndiyo amfundishe hili.

Mara nyingi wasichana wana majaribu ya kuzungumza mno ubaya wa wengine na kusifia kwa kutia chumvi (flattery). Kama wazazi tuepuke kutia chumvi, uongo, umbeya, manung'uniko, wivu, hasira, kiburi na unafiki kwa maneno, matendo na mwelekeo. Mpeleke amhoji mtu kanisani "Kwa nini unamwamini fulani na si Fulani?" Je, waweza kumwamini binti akisema kitu

au anasema nusu ukweli na nusu uongo akitoa udhuru? Je, anasema uongo kwa matendo yake na kutunga hadithi, au kupunguza kweli? Je, anatunza ahadi zake? Je, akisema uongo anajaribu kuufunika uongo huo kwa uongo mwingine? Je, anazungumza watu vibaya wasipokuwepo? Je, anarudisha vitu alivyoazima? Je, ana uaminifu katika mahusiano, magoli, malengo au mipango yake au anajidanganya hata yeyé mwenyewe? Je, anapenda kutoa rushwa au kujipendekeza ili afanyiwe kila anachotaka? Je, anasema kwamba alikuwa 'anatania tu' akikutwa amefanya uovu? Je, mara nyingine anazungumza bila kufikiri na kukosoa wengine bila kujali au kuwa na upole? Je, yupo huru kuja kwako na kukueleza mambo yasipokuwa mazuri na hasa yale nyeti?

Jadili naye maswali kama 'Kwa nini si vizuri mke kumsema vibaya mume, wazazi au hata wenzake kwa watu? Kwanini mwanafunzi hapaswi kumzungumza vibaya mwalimu wake?' Uaminifu ni muhimu utotoni na hata ukubwani. Jadilini ubaya wa talaka na aandike insha.

Je, yupo tayari kumsaidia rafiki endapo amekosea kwa upendo na unyenyekevu, na siyo tu kumsema mbele ya watu na kumwacha aendelee na tabia mbovu? Je, anakasirika haraka na kufuta urafiki kirahisi. Je, anapenda wote wasiwe na urafiki na yule ambaye yeye ameacha kuwa rafiki naye? Je, anasamehe haraka akiwa amekosewa? Je, anathamini mawazo ya marafiki zake au wadogo zake, na kuwasimamia naye pia aweza kuwapa ushauri mzuri?. Je, anakuwa na wivu au chuki rafiki yake au ndugu akifanikiwa? Je, yuko tayari marafiki zake wawe marafiki wa wengine, au anataka wawe marafiki zake tu? Je, anapenda kuwazomea, kuwashushua au kuwabeza wengine akiwa na marafiki zake? Je, anathamini uongozi wa wazazi na magoli ya familia. Je, anakosa adabu kwa wazazi wake mbele ya marafiki zake?. Je, ana uaminifu kwa mume wake wa siku za usoni kwa kujitunza au huingilia urafiki wa kimapenzi na wavulana/wanaume? Je, anajua kwamba ndoa ni jukumu la maisha yote (lifetime commitment)?

Kama msichana, usikivu ni jambo jema, hata kwa mume atakapoolewa. Kuwa msikivu bila kuingilia kati, kubishana au kupayuka payuka lisiwe lengo lake. Anapaswa kujua mke anamsikiliza mumewe kama kiongozi, akitoa majukumu au kujadili mambo ya familia. Watoto wake pia watahitaji kusikilizwa, hii ni karama anayopaswa kujifunza kuwa nayo. Wanawake wengi twahitaji tusikilize zaidi ya kuzungumza.

Dhambi zinazotuzinga kwa upesi kama vile umbeya, kukosoa, na kutona tona (nagging) zinatokana na kuzungumza sana badala ya kusikiliza. Twapaswa kufundisha mabinti zetu kusikiliza. Kitabu cha Mithali, Mhubiri, Zaburi na barua za Paulo vina mengi kuhusu haya. Angalia watu ambao unafikiri wana hekima, kisha waangalie wakizungumza na watu. Je, wanazungumzaje, wanasikilizaje? Je, wanaulizaje maswali? Je, waweza kujifunza nini toka kwao? Umbeya na kutosikiliza vizuri vina undugu. Je kwa nini ni muhimu mke kumsikiliza mume au mtoto kabla ya kurukia? Mwambie aandike insha ya kumsikiliza mume au mtoto. chukua tangazo la biashara au andika na kisha umpe alitoe kasoro.

Maswali ya kujiuliza kama mzazi ni: Je, anasikiliza sauti ya Mungu na kumtii Roho wa Mungu anapozungumza na moyo wake? Je, anasikiliza mahubiri kwenye nyumba ya ibada? Je, anaweza akarudia yaliyozungumzwa ibadani au anasema mahubiri yalikuwa mazuri, bali hawezi kukumbuka kitu? Je, anakusikiliza wewe au baba yake mkizungumza naye? Je, anaonyesha adabu

ukizungumza naye, Je, anajifanya hakusikia? Je, anapoteza mawazo kwingine watu wakizungumza naye? Je, hana simile ukizungumza naye na anataka aendelee na shughuli zake, na mara nyingine anaondoka ukiendelea kuzungumza? Je, anasikiliza kwa umakini unachomwambia na kukifanya sawa? Je, anakumbuka alichoambiwa? Je, anapenda kuingilia kati mazungumzo na kufikiria atakachosema badala ya kusikiliza? Je, anatoa ushauri wake haraka wakati bado mwenzake anamwambia tatizo lake, Je anapenda kutawala mazungumzo yote?

Kama msichana anatakiwa awe na sifa ya upendo, asiwe mtu wa kujifikiria mwenyewe; na akariri fungu la1 Korintho13: 4-8, na baada ya wiki mbili hivi amalize kukariri yote. Je, akipenda watu ni matendo gani atatenda? Je, akimpenda Mungu na kutaka kufanya mapenzi yake ni matendo gani yataonekana kwake? Je, awezaje kuwaonyesha upendo ndugu zake, baba na mama yake, babu na bibi, Wajomba na shangazi? Je, apaswaje kuwatendea “maadui” zake, kutokana na Neno la Mungu?

Tito mbili yahimiza wanawake wajane wazee kufundisha wanawake vijana kupenda waume zao. Upendo unafundishwa pia, na ni vyema tuwafundishe binti zetu, hasa katika ulimwengu wa leo uliojaa ubinafsi au umimi (me, myself, and I). Wengi wanasema nafanya hili kwa ajili yangu, au “kila mara nawafanyia watu vitu, nimechoka sasa nataka nami nijifanyie!”. Wanawake wajane, wanathamini sana waume zao, hasa wakiwakumbuka, wanasema ‘ningejua’.

Someni pamoja na kujadili upendo wa aina tatu (Phileo yaani wa ndugu, Agape yaani wa Mungu na Eros yaani wa mapenzi kati ya mume na mke). Je hizi aina za upendo zinatofautianaje?. Je, ana uvumilivu wengine wanapokosea au anapata hasira haraka? Je anaonyesha upendo wa Mungu kwa wengine hata kama haafikiani nao? Je, yupo tayari kusahau makosa madogo madogo ya watu aliyofanyiwa? Je, anapatana na kushirikiana na wengine, na wengine wanapenda awe rafiki yao? Je, anapenda kusaidia mahitaji ya wengine kabla yake au anajitafutia yeye kwanza kabla ya ndugu zake au marafiki? Je, anakimbilia kiti kizuri au andazi kubwa au mwanasesere mzuri ili wengine wasipate? Je, anaangalia mapungufu ya watu na udhaifu wao kupita kiasi? Je, anawakosoa marafiki zake kwenye kadamnasi? Je, anapenda kujenga wengine au anapenda kujipigia filimbi yake na kujisifu? Je, anakumbuka makosa ya wengine mara kwa mara? Je, anacheka na kufurahi wengine wakipata adhabu? Je, anatafuta nafasi ya kuhudumia wengine au anataka yeye tu ndiye ahudumiwe? Je, anaonyesha upendo kwa wale wanaotaka kumdhuru au kumwangusha?

Utii na kuwa na adabu ni muhimu sana kwa msichana. Binti zetu tuwatayarishe wamtii Mungu. Ili kuishi maisha ya amani na furaha, ni muhimu kumtii mume endapo Mungu amewapangia kuolewa. Mabishano, kukunja nyuso saa yote, manung’uniko, kuzira, na kutaka kuburuza wengine si tabia njema. Wote tumeanguka na kupungukiwa na utukufu wa Mungu ila tunyanyuke.

Mama yetu Hawa kwa kutotii na kukaa karibu na mume wake, alikuwa mtenda dhambi kwa kwanza duniani. Mara nyingi tunafikiri wanaume wana vituko vingi na dhambi nyingi kama vile kuua, ujambazi, uongo, na mengineyo; bali tukumbuke ni mwanamke ndiye aliyetufikisha hapa kwa kutotii! Mwanamume naye amepewa sehemu yake, ya kumpenda mke wake kama Kristo alivyolipenda kanisa na kulifia. Hii ni kazi kubwa mno pengine kuliko ya mwanamke akiitenda inavyopaswa.

Nilimsikia mama mmoja akisema wanaume wana ukarimu mkubwa kuliko wanawake, na hivyo tunapokuza watoto wa kiume tusisahau hili. Nilishangaa baadaye nikagundua ni kweli kwani mipango yote ya serikali ya kutoa misaada aidha ya ustawi wa jamii au kwa mataifa mengine, wanaume ndiyo wahusika mara nyingi! Hivyo wakina mama, tufundishe mabinti zetu ukarimu na karama tofauti za jinsia na fundisho litafika kwa wajukuu zetu pia! Kwa upande mwingine hasi, wanawake wanagombana na watu hapa na pale au majirani bali wanaume wanaenda vitani na kugombana na wengi! Haya yote mwanamke wa mithali 31 apaswa ajue ili asaidie watoto wake wote. Wanasema Barbara mke wa Bush yule mzee aliyekuwa raisi, alisema haya wakati mtoto wake aliposhika uraisi wa Marekani, nchi yenye nguvu duniani 'nimetawala dunia mara mbili, kwanza mume wangu alikuwa raisi, kisha mtoto wangu wa kiume sasa ni raisi!'. Mama huyu alijua kama mama ana nafasi fulani, si lazima ile mwanamume alipewa, ila ana fungu lake.

Katika kielelezo alichotupa Mungu, si kazi kumtii mume, kwani yaonekana yeye ndiye mwenye jukumu kubwa katika ndoa nasi ni wasaidizi. Kumtii mume ni furaha kubwa na ni amri toka kwa Mungu, na kama huamini, basi mwulize mama mwenye mkamwana (mke wa kijana wake) asiyemheshimu akueleze jinsi serikali hiyo ilivyo na masikitiko yake.

Mtoto wa kike anapaswa kujua agizo la Mungu la waefeso sita "Enyi watoto watiini wazazi wenu katika Bwana maana hii ndiyo haki". Je, ni njia gani binti aweza kuonyesha utii kwa wazazi wake? Je, mamlaka gani mengine zaidi ya wazazi anapaswa kutii? Kanisa, serikali, kazi n.k. Someni Neno la Mungu la wale waliotii na wale wasiotii kama Akani, Kaini, Nuhu, au Yakobo. Soma kumbukumbu la Torati 28.

Je, kwa nini Jina la Mungu linaweza kutukwana kwa mtoto asiyemtii mzazi au mke asiyemtii mume? Je, anatii bila kusita, kubishana au kulalamika? Je, anafanya unachomwambia kwa furaha au anaweka sura mbaya? Je, uso wake waonyesha roho ya unyenyekevu mbele ya Mungu na mamlaka Mungu aliyoweka kwa ajili ya maisha yake? Je, matendo yake yanaonyesha utii? Je, anatii mamlaka uliyompa mwingine kama yaya, shangazi au mwalimu? Je, anajua kwamba Mungu Ndiye mamlaka ya mwisho? Je, anathamini maamuzi yako hata kama mara nyingine hayaleti maana kwake? Je, anajua jinsi ya kukata rufaa kwako kwa adabu endapo anataka asikilizwe tena? Je, anaonyesha adabu kwa polisi, walimu na mamlaka ya serikali? Je, anatumia muda kujua Neno la Mungu na kulitii? Je, anakutii ukiwa karibu au hata mbali ambako humuoni? Je, anatii kwa furaha au kwa moyo mzito?

Kutunza amani nyumbani ni muhimu kwa msichana. Usichana ni maabara ya vile atakavyofanya duniani. Mahusiano mema ni zawadi toka kwa Mungu na kuyatunza na kuyapalilia ni jukumu. Tuwaepushe mabinti zetu na kuzira, kuweka visasi kwa wazazi au vinyongo kwa ndugu zao. Kuwa na chuki au hila si kitu Chema. Twapaswa tusamehe ili kuleta uponyaji na kukua na hata kukomaa kiroho. Soma kuhusu upatanishi, magomvi, kuonywa, na mwanamke mgomvi kwenye kitabu cha Mithali.

Je, adui atendewaje? Mpe binti aandike kuhusu kusamehe wengine na kusamehewa. Soma Neno la Mungu na kuona mifano ya kusamehe na kusamehehwa. Twaweza kujua Neno la Mungu, bali tusipojua kusamehe tutapata

maumivu mengi, mahusiano yaliyovunjika na hata kwenda Jehanamu tusipotilia makini. Mahusiano ya binti akiwa mdogo katika familia yanamtayarisha kuwa na mahusiano mema na familia yake atakapokuwa mtu mzima.

Je, wazazi ni watu wa kupatanisha wengine, Je, wanasamehe watu, au wanapenda malumbano? Wewe kama mama angalia pale unapaswa kusahihisha. Jadilini kuhusu mwanamke mgomvi kwenye kitabu cha Mithali. Soma pale wanawake waligombana kwenye Biblia kama vile Sara/Hajiri, Raheli/Lea/Yakobo, Penina/Hana, Mikali/Daudi. Miriamu/Musa, Ayubu/Mkewe uodia/sintike. Waligombania nini? Matokeo yake yalikuwa yapi? Je, tunajifunza nini?

Soma Waebrania 12:15-16 na Jadili na binti. Jadilini kuhusu hasira, visasi, kusamehe na uvumilivu.
Je, anachukuliana vizuri na ndugu zake au kila mara wanagombana akijitetea kwamba anatunza haki yake? Je, ana haraka ya kuzungumza au anasikiliza anapoonywa? Je, anapogombana, anachunguza moyo wake kama ni yeye ana makosa? Je, anasamehe wengine, akijua hata yeye ana makosa pia?

Je, yupo tayari kumfuata aliyemkosea na kumwomba msamaha? Je, anapenda upatanisho au anakaa na kisasi? Je, anajua jinsi ya kutafuta suluhisho kwa njia ambayo haitaleta ugomvi? Je, anasali kwanza kabla ya kuzungumzia upatanisho? Je, yupo tayari kusuluhishwa hata ikibidi zaidi ya mara moja na mtu huyo huyo? Je, anajaribu apatane na waliyekosana mapema au anakaa na hasira muda mrefu? Je, anaamini Mungu atampigania au anapenda kuchukua sheria au kisasi mkono mwake? Je, anaangalia mazuri ya wangine au anaangalia mabaya yao tu? Je, ni mwepesi kukosoa na kukaa na chuki? Je, anasamehe na kusonga mbele au anapenda kuyaleta yale aliyokosewa zamani tena na tena?

Haya ni muhimu kwani binti akiwa na nyumba yake atakosewa na mume au watoto, naye atawakosea pia. Hivyo aanze kujifunza mahusiano ya kutunza amani anapokua.

Lazima ajue unyenyekevu ni jambo muhimu. Kunyenyekea kwa uongozi wa Mungu ili kila siku umimi upungue kusudi Roho wa Mungu aweze kufanya kazi ya kumsaidia kwa tabia njema. Awe tayari kukosolewa bila kubishana. Je, yuko tayari kusema alilokosea bila kuficha? Je, maneno yake yanaonyesha kiburi na anafikiri wakati wote yeye ndiyo yuko sawa? Je, hakati tamaa akifanya dhambi bali yupo tayari kuomba msahama si kwa kuepuka adhabu bali kwa kumpenda Mungu. Je, anajua hawezi akafanya vizuri bila uongozi wa Mungu? Je, anajua kwamba Mungu ndiyo mtawala na amempatia wewe mzazi, umsaidie katika maisha yake? Je, anajua sheria za Mungu ni kwa ajili ya mema kwetu?

Kuishi maisha ya usafi ni muhimu kwa binti, na mji wake atakapokuwa mtu mzima. Usafi wa mawazo, maneno na matendo. Mfundishe kuomba kila siku ili aweze kumtii Mungu na kuepuka majaribu.

Je, majaribu ni nini? Kwa nini tunafanya dhambi, matokeo ya dhambi ni nini? Someni pamoja kwenye Neno kuhusu dhambi na maisha ya giza au mahusiano ya dhambi. Je, wangapi wamefanya dhambi? Mshahara wa dhambi ni nini? Je, ni kina nani walishinda majaribu? Na ni kina nani waliepuka? Someni pamoja Mithali saba na jinsi ya kuepuka tabia ya mwanamke mgeni? Je, anajua kwamba kuna mapambano kati ya Shetani na Mungu na kwamba yeye anahusika? Je, anajua shetani alitoka wapi? Je, anajua akiwa na shida hapaswi kwenda kwa waganga au wachawi bali kwa wacha Mungu? Je, anajua yeye yuko

hapa duniani kwa sababu gani?, Je, anajua jinsi atakavyopata ushindi? Je, anajua kulitumua Neno la Mungu kupata ushindi kwa majaribu? Je, anaepuka mahali kwenye mitego ya majaribu au anajipeleka? Je, anachagua marafiki wanaompenda Mungu au wale wanaompeleka kwenye uovu? Je anajua kukimbia majaribu? Je, anakubali mashauri kuhusiana na marafiki wabaya? Je, anakutii katika mambo yote kama vile muda wa kurudi nyumbani au shughuli za za kufanya?

Je, ana tabia ya kutongoza wavulana au kusema vimaneno vyenye walakini vinavyowafanya watu wamshuku mambo maovu? Je, anamwomba Mungu kumsaidia kuepuka dhambi, Je, anaepuka marafiki wa kiume 'boyfriend' na kujua mpango huo wa dating si wa usafi bali ule wa uchumba (courtship)? Je, anatumia muda wake vizuri au anasoma vitabu vichafu au kuangalia picha mbaya? Je anatumia muda wake kuwa na ndoto za mchana zisizo na faida? Je, anakuja kwako kwa maswali ambayo ni nyeti na ya rika yake au anakuogopa (ya uchumba, marafiki wabaya n.k)?

Ni vyema kufundisha mabinti wetu uvumilivu na kuwa na tabia ya mbinguni. Twawafundisha haya wakiwa wadogo kabla ya kupevuka. Wawe na uvumilivu katika mambo mengi, mfano ya kutoanza kuwa na marafiki wa kiume mapema bali kufuata mpango a uchumba. Hatushauri kuanza uchumba mpaka kupevuka, hii ni kuanzia miaka 18, ila ni vyema waweze kujitegemea ili wasiwe mzigo. Marafiki wa kawaida (general friends) ndiyo wale ambao mara nyingi ataolewa nao.

Aepuke kuzungumza na wavulana mafichoni, akiwapa matumaini fulani ya urafiki usio mzuri. Ni vyema awe wazi ya yale yanayoendelea kwa vile wazazi wana uzoefu mkubwa, hasa maisha ya leo katika kuwasadiia mabinti ili wasiingie katika ndoa zenye huzuni. Mama uwe tayari kujadili; mtoto wako hawezi kujifunza kwa mwingine sawa, ila kwako. Ni vyema mama amsaidie binti kuweka viwango vya mume anayetaka kuolewa naye, akiwa tayari kutii na kumheshimu mume huyo. Angalia mifano ya Isaka/Rebeka, David/Mikali, Esau, Samson, Solomon, .

Soma vitabu kama, "I Kissed Dating goodbye;" by Joshua Harris na mjadiliane hatari za Dating (urafiki na wavulana) na uzuri wa Courtship (uchumba). Je, yupo tayari kusikiliza mashauri yako kuhusu kuchagua mwenzi wa maisha, Je, anaamimi kwamba Mungu atamsaidia kupata mchumba au anataka kuharakisha? Je, yupo tayari kukua kiroho ili kuwa na nyumba bora au anakimbilia aolewe? Je, anasoma hadithi za mapenzi ambazo zote zina mafundisho mengi ya uongo kuhusu upendo na ndoa?

Je, yupo tayari kujitunza kwa kuepuka majaribu ya ngono yaliyo katika miziki, vitabu, picha, marafiki na filamu? Je, amekuja kwako na kuuliza maswali kuhusu ngono kwa mpango wa Mungu na ngono safi? Je anajua mpango wa Mungu kuhusu ngono? Je, ameelewa kukomaa kwa msichana kwa kuvunja uongo na jinsi ya kujitunza? Chukua muda kuzungumza nayo haya, si mara moja tu, ila hapa na pale. Je, yupo tayari kuishi peke yake maisha yake yote kama ni mwito ambao Mungu amemwitia?

Kujitoa kikamilifu ni muhimu kwa msichana. Twaona maisha ya Ruthu jinsi alivyojitoa kwa mume wake, na kisha kwa familia ya mume wake na kubarikiwa. Binti anapaswa aheshimu wazazi wake akiwa mdogo nyumbani kwao. Awaheshimu ndugu na jamaa kama kaka, dada, mama, baba, babu bibi, mjomba na shangazi. Mwangalie na mfundishe kwa makini, kisha ujiulize

haya. Je, anaheshimu wakubwa wake? Je, anawakejeli, au kuwapuuzia wakubwa wake? Je, anataka bibi na babu wamsaidie yeye bali yeye hataki kuwafanyia kitu? Je,anasikiliza kwa adabu wajomba, baba wadogo, au shangazi zake? Je, anatawaita bibi na babu nakuomba mashauri yao? Je, kwa kawaida anawasiliana na babu na bibi? Hapa wazazi ni lazima tuonyeshe mfano wa kupenda na kuheshimu wazazi wetu. Je, anawasaidia wazee kijijini mwake kwa furaha? Je, anawashukuru ndugu na jamaa wanapomsaidia au anaona ni haki yake?

"Hutafuta sufu za kitani, hufanya kazi yake ya mikono ka moyo" Fungu la13. Twapaswa kuwafunza mabinti zetu kuwa na ujasiliamali au bidii ya kazi. "Asiyefanya kazi na asile." Wanapaswa wafanye kazi, wakijisia au wasipojisikia! Wajifunze kufanya kazi kwa furaha, kazi ni amri toka kwa Mwenyezi Mungu kabla hata ya maanguko ya binadamu. Mfanyakazi awepo au asiwepo, binti ajue kufanya kazi zote na azifanye.

Binti afanye kazi za mikono, kazi za shule, lazima tuwe na orodha ya vitu vya kufanya kila siku. Kama ni kulisha kuku, kutandika kitanda, kufua, kufagia, kudeki, kulisha wanyama. Twajifunza toka kwa nyuki, siafu na wanyama wengine kuhusu kutokuwa na uvivu. Chukua muda kuona wadudu hawa na binti. Aangalie unavyofanya kazi, naye afanye akijali wakati atakapojifunza kuzifanya asifanye kivivu. Mpe kazi zingine kwa malipo madogo ambazo si za kila siku kama una uwezo kumpa motisha. Aweza hata kufungua akaunti yake kama familia inaweza kufanya hilo na kujifunza kutunza akiba/kutumia pesa kwa hekima. Someni kuhusu kulala kupita kiasi na hasara zake. Chunguza maisha ya Yusufu, Nehemia, Daniel , Ruth au Tabitha. Angalia maisha ya Raheli na Rebeka wakifanya kazi kabla ya kuchumbiwa. Mkatie sehemu ya bustani ashughulikie. Angalia maisha ya wanariadha, wanasayansi, waandishi, wavumbuzi na masaa waliyotumia. Angalieni wanawake wenye bidii mnaowajua, wanafanya mambo gani? Je, uvivu una shida gani?

Jiulize, Je, anafanya vizuri anavyoweza? Je, anafanya kazi pale watu wanapomwangalia, Je, analalamika na kuweka sura mbaya akitaka apewe zawadi au kulipwa? Je, anangojea mwingine afanye kazi, aking'unung'unika au kutoa vijisababu? Je, anauliza maswali kana kwamba hajui kufanya kazi uliyompa, au inakuwa sababu kwake ya uvivu? Je, anafanya kazi za kila siku bila kukumbushwa? Je, anamaliza kazi au anapotea au kupeleka mawazo pengine? Je, waweza kumweleza jinsi kazi inavyofanywa na akaifanya? Je, anafanya kazi nusu nusu? Je, anatunza vitu vyake? Je, anarudisha vitu vyake baada ya kutuvimia? Je, anacheki kazi yake kabla ya kuripoti au anaparaza paraza tu? anapoteza muda, au kusema nitafanya kesho? Je, anakata tamaa na kuacha kufanya kazi inapokuwa ngumu?

"Afanana na merikebu za biashara, huleta chakula chake kutoka mbali, tena huamka kabla haujaisha usiku;" fungu la 14. Tabia ya uzalishaji mali, bidii ya kazi na utunzaji wa mali ni muhimu sana. Mtoto wa kike afundishwe bidii ya kazi za mikono, jinsi ya kutunza pesa, jinsi ya kufanya bajeti, jinsi ya kununua vitu sokoni au dukani. Kama kuna uwezekano alinganishe bei kadhaa au masoko tofauti kabala ya kununua. Afunzwe ubaya wa ubaradhifu au utumiaji mbaya wa vitu kwa kufuja. Ajue jinsi ya kununua chakula chenye lishe bali chenye bei nafuu. Afundishwe uchuuzi, kuona thamani ya kitu na kuweza kuzungumza apunguziwe kama inawezekana (bargain). Je, akinunua vitu kwa jumla, au vingi bei inakuwa ndogo au kubwa? Je, akipika chakula kingi akigawe mara mbili kwa kutumia siku

moja, Je, inasaidia matumizi ya pesa?

Mfundishe jinsi ya kununua , afanyeje ili aweze kuweka akiba? Afundishwe kufanya bustani ili kupunguza makali ya kununua kila kitu, hasa mboga. Je, anajua kutafuta nguo za mitumba zilizo nzuri na za kuzimachisa vizuri zipendeze, aidha kwake au kwa wadogo zake? Familia nyingi zinaingia gharama kwa burudani (recreation) ambazo ni ghali, je anajua burudani za kufaa na zisizo na gharama?

Niliona pale Dar es Salaam familia za wahindi wanaenda baharini kupunga upepo, na kula chips za mihogo au madafu kwa bei nzuri. Wakati familia nyingine zinaenda kwenye burudani ambazo ni ghali mno wakila kuku wa kukaanga kwenye hoteli kubwa soda, pizza, icecream na vyakula vingine Ghali, na ambavyo siyo vya afya. Haya yote ni muhimu kuwafundisha watoto wetu.

Je, chakula kinachobakia anaweza kukitunza na kukitengeneza vizuri kifae? Mabaki ya mboga, na maharage machache, aweza kutengeneza supu na kuongeza vitu vingine. Je, wageni wakitokezea ghafla anajua jinsi ya kuongeza chakula kidogo kitoshe wengi? Afundishwe kufuga kuku wa mayai au ng'ombe wa maziwa kama kuna uwezekano. Msichana afundishwe kutunza chakula kwa wakati wa kiangazi.

Zamani makabila mengi yalikausha mboga za majani, viazi vitamu n.k. siku hizi hatufahamu haya. Wakati wa mvua tuna mboga nyingi, ila wakati wa kiangazi tunapata shida. Angalia kama ananunua visivyohitajika bila kufikiri. Je, anakubali matangazo ya biashara ya kununua vitu kirahisi? Je, yupo tayari kununua vitu ambavyo vimeshuka bei, au ana uvumilivu wa kungoja? Je, anajifunza kushona, kufuma na ustadi mwingine kupunguza matumizi? Je, ukimtuma sokoni, anaweza kulinganisha bei na kuleta vitu vya nafuu na vizuri. Je, ukimwandikia orodha ya vitu vya kununua dukani, anavifuata, au ananunua usivyomtuma? Je, akiingia sokoni anajua tofauti kati ya vyakula vya lishe bora na vyakula visivyo na lishe (junk food-vyakula ovyo) Je, anaweza kufuata bajeti na kuitumia? Je, anaacha acha vitu vyake bila kujali viharibike?

Msichana afundishwe jinsi ya kutumia muda vizuri. Muda ni talanta ya ajabu, ambayo kila mtu amepewa. Mtoto afundishwe jinsi ya kumudu muda na kukomboa wakati ili aweze kumsaidia mume wake, watoto, jumuiya na kanisa. Mfundishe jinsi ya kupanga muda katika kufanya kazi za nyumbani. Mpe mradi wenye muda wa kumaliza (deadline). Tengeneza naye orodha ya mambo ambayo mnayoweza kumaliza kwa dakika tano, kumi na kumi na tano. Talanta ya muda ina thamani kubwa.

Atembee na kitabu anapokuwa anangojea basi, afume au afanye jambo fulani. Vitabu vya kumsaidia kimaisha (long life learning). Angalia jinsi muda ulivyoikuwa muhimu katika uumbaji kwenye Mwanzo moja. Tengezeni ratiba ya kutumia kwa siku nzima, mfano kuamka, kupiga mswaki na kuoga, kusoma Neno la Mungu. Mpatie muda awahoji watu wazima kwamba wangerudi nyumba ujanani ni nini wangefanya tofauti.

Je, majuto gani ya kupoteza muda au kutofanya jambo? Je, ni (mkato) short cut gani zatakiwa ukipika, ukisafisha nyumba au ukishona? Je, ni jinsi gani mtu abajeti muda wake? Je, wafuatao walitumiaje mida yao kwa hekima? Daudi, Josiah? Kristo? Daniel, Miriam, Yusufu, Musa, Samueli. List shughuli ambazo zinafanyika kwa kipindi fulani tu katika maisha ya msichana mfano elimu, kuzaa

watoto, ndoa, uzeeni. Mwulize kama anafanya yanayotakiwa kwa wakati wake.

Nunua daftari la kupanga muda na kalenda ya mwezi mirejee kila wiki. Jiulize kama anatumia muda wake vizuri kupanga maisha ya baadaye au ni kucheza na kupoteza muda. Je, anatumia muda kuwekeza kwenye umilele kwa kusoma Neno la Mungu na kuomba. Je, ana ratiba ya kila siku au anakaa na kuwaza ndoto za mchana. Je, muda wake wa mapumziko anatumia vizuri? Je, apoteza muda kwenye simu, tv na Kompyuta? Je, akipewa kazi anapoteza muda au anatunza muda? Je, anachukua muda mwingi kujirembesha? Je, analala, ana ratiba anayoifuata. Je, anawahi kanisani na shuleni au miadi nyingine? Je, anapenda kusema nitafanya kesho au kungoja kufanya mambo dakika ya mwisho? Je, anaweza kufanya shughuli mbili au tatu kwa wakati mmoja au akingojea maharage yaive, anakaa hapo hapo kisha ndiyo anainjika mboga? Je, angaalia njia za faida za kutumia muda wake kwa hekima?

Kama msichana na baadaye mama mwenye kushugulikia mume na watoto, ni vyema ajue kufua nguo, kujitunza kwa usafi katika mambo yote ya kike, kupika, kukomaa na shughuli zote za nyumbani. Je, anaweza kugawa majukumu kwa wadogo zake, na hatimaye hata akiwa na msaidizi wa kazi aweza kumwambia cha kufanya bila kupoteza muda? Aangalie jinsi ufanyavyo kazi na kuzigawa kwa wengine wakusaidie. Angalia vifaa ambavyo unafanyia kazi na mwelimishe, naye aanze kununua pole pole anapopata visenti. Vifaa hivi ni kama cherehani, sindano, jembe, masufuria n.k.

Je, anajua kutumia cherehani, na hata kukarabati nguo zake? Je, anajua kutumia sindano, kukarabati nguo, kushona vifungo, au kufuma vitambaa. Je, anaweza kusoma pattern ya sweta, kitambaa cha kufuma, au nguo ya kushona?

Chukua pamoja na binti yako mradi fulani mfano kupamba ukumbi wa harusi na andikeni jinsi mtakavyofanya shughuli hatua kwa hatua na kuimaliza.

Angalia maisha ya Yusufu, Debora na Daniel. Je, Mungu aliwatayarishaje ili waweze kuwa watawala? Mungu anatayarisha wasichana wetu kuchukua majukumu ya kutunza familia zao na mengineyo. Angalia kama anamaliza shughuli unazompa. Je, aweza kuivunja project kubwa kwenye kazi ndogo ndogo na kuwapa wengine wamsaidie? (delegation), Je, anafundisha wadogo zake kwa uvumilivu?, Je, anapopewa kazi ya kusaidiana na wengine, anataka aifanye yeye mwenyewe? Je, anaweza kuelewa maelekezo ukimpa (directions). Je, aweza kukagua kazi ya wengine ambao wako chini yake? Je, anaongoza wengine kwa unyenyekevu au anawakandamiza na kuonyesha kwamba yeye ndiye bosi? Je, anasaidiana na wadogo zake kufanya kazi au anawatazama tu? Je, wengine wanapenda kufanya kazi naye au wanamuepa?

Mwanamke anaweza kupika milo 1000 kwa mwaka, wengi wanakumbuka vyakula vya mama zao. Ni muhimu tuwafundishe watoto wetu kupika vizuri. Tujifunze hata na mapishi mengine ya makabila tofauti na kupanga vya kupika, kutoka kwa vile tunavyolima na vile ambavyo ni rahisi kwa msimu ule. Je, anajua kiasi gani kila mtu katika familia anapaswa kula? Siku hizi za utandawazi aweza kupata mapishi toka sehemu mbali mbali kama vitabu, tovuti na mengineyo. Je, mwaweza na yeye mwandike kitabu chenu cha mapishi rahisi cha kutumia na kanisa lenu?

Wataalam wanasema kwamba mapishi yoyote yakiwa na zaidi ya vitu saba si mema kwa afya. Mfundishe kupika,si kwa vikolezo vingi ila kwa afya, kisha

ladha na baadaye mwonekano. Kuna mapishi yayonachukua muda mfupi kupika, mengine yanachukua pesa chache. Ulizia marafiki, makanisani na ndugu mapishi mapya, na yakusanye muyaandike. Mwaweza kujitolea kanisa lenu kuwa na darasa la upishi kila mwezi mara moja kwa masaa matatu hivi.

Je, vifaa gani vyahitajika kwa pishi. Je, mwaweza kujifunza kupika mikate, kutengeneza jam au peanut butter? Angalieni magazeti ya upishi. Hoji wakina mama "Kwa nini wakati wa kula ni muhimu?" Je, anajua kuoka? Kukaanga? Kuchemsha? Je, anaweza kutumia vifaa vya jikoni kwa ustadi, usalama, na kuvitunza vizuri? Je, anaweza kufuata maelekezo ya mapishi (recipe) fulani? Je, anaweza kupikia watu wakiongezeka mara mbili? (Mfano ugali wa watu sita badala ya watatu). Je, aweza kupika kwa wakati na kutenga chakula mezani? Je, anajuaje chakula kimeiva? Je, anasafisha vyombo alivyotumia baada ya mapishi?

Je, mama akiumwa anaweza kumudu mambo yote mwenyewe? Je, anaweza kutengeneza chakula kitamu na cha kupendeza? Je, wale anaowapikia ni muhimu kuliko chakula anachotengeneza? Je, anapenda vyakula ghali vya mapambo mengi badala ya kubana matumizi na kupika vyakula vyenye lishe? Je, anaweza kubajeti chakula cha mwezi. Je, anakusanya mapishi mazuri na kujifunza yale yanayowezekana? Je, anajua kuwapikia watu wenye shida maalumu za afya kama kisukari, allergy, moyo au presha? Je, anapenda kuendeleza talanta ya kupika na kuuza chakula? Kama mama je, upo tayari kumsaidia muanze genge dogo (restaurant)? Je, mambo gani ni muhimu yahusuyo chakula mbali na kwamba kina lishe nzuri na kina ladha tamu?

Mambo mengine ya kuangalia ni kupangilia mambo. Fungu la 15. Kupanga nyumba vizuri, kunaleta mawazo kutulia, na pia kunaakisi tabia ya Mungu ambaye ni wa mipango na uzuri (beauty). Tunaowaalika wanapenda waje zaidi kama nyumba zetu zina utulivu na mipangilio. Binti aliyejifunza kupanga vitu akiwa mdogo atakuwa msaada kwenye familia yake na hata atakapofanyia kazi.

Watu wengine wanazaliwa na talanta ya kupanga vitu vizuri, kama wanawake wa mashariki ya mbali, wanapangilia maua vizuri bila kutoka jasho sana; ila wengi wetu tunahitaji kufundishwa na kuhimizwa tena na tena. Kama wewe mama si mpangiliaji mzuri wa mambo, kama mimi, tafuta msaada kwa kusoma na kwa wengine.

Sheria ya kwanza mbinguni ni mpangilio (order). 1Kor:14:40 yasema kila kitu kifanyike kwa mipango. Mabinti wadogo wakicheza warudishe vitu vyao. Wajifunze kutandika vitanda vyao. Asubuhi mpange siku yenu na hata kuandika, mnavyotaka kufanya, la sivyo siku itaisha bila kufanya mengine. Jifunzeni jinsi ya kupangilia mipango yenu kwenye kalenda, au daftari. Wafundishe watoto kupanga vitabu vyao, picha, wanasesere, meza za kusomea, barua, kazi za shuleni, n.k. Wafundishe kupanga magoli, ya muda mrefu na mfupi.

Panga nao jiko, makabati yao, makabati ya vitabu. Pangeni pamoja na kuwafundisha jinsi ya kutoa kipaumbele (priority) katika mipango. Mkitaka kwenda mahali, kama safari pangeni pamoja, vitu vya kuchukua, ramani, kubook hoteli, simu zinazohitajika, tarehe za kwenda, mahali pa kupita, na vitu vya kufanya. Panga na mtoto ratiba ya siku ya kukaribisha wageni au karamu ndogo. Wekeni bajeti na jinsi ya kuifuata. Pangeni michezo, mapambo, na jinsi ya kupata pesa za kufanya hii karamu. Mkiweza someni vitabu vya Don Aslets "Clutter's Last Stand" au "Clutter free".

Tembeleeni nyumba za wanawake waliopanga vitu vizuri na kwa idhini yao tazameni jinsi wanavyopanga jiko, makabati, au sebule. Pangeni pamoja rekodi za nyumbani za afya, kama chanjo, huduma ya kwanza, na miadi (appointments) ya kumwona daktari. Pia vyeti, kama vya kuzaliwa (birth certificate), ripoti zao za shule, viweke mahali maalum.

Chukueni faili jipya na kugawanya sehemu na kuandika namba za simu na address za watu, appointment za kalenda kama michezo/matukio, maelekezo kwa yaya, size za nguo za watoto wa nyumbani. Kila moja kwenye ukurasa wake. Weka hichi kitabu mahali mnapoweza kukipata na kukirejelea (refer). Angalieni mahali nyumbani ambapo hapa mipangilio na kufanya pamoja baada ya kupanga la kufanya.

Mpe binti kazi ya kuweka picha vizuri na kuzilebo kwenye photo album. Pangeni pamoja risiti, marakaratasi ya bima au picha za kufundishia kanisani. saidiana na binti kupanga chumba chake na kukipamba kwa bei isiyokuwa kubwa. Soma www.Titus2.com wameandika kuhusu kumudu kusimamia nyumba (managers of their home). Mwambie binti aandike insha ya "Thamani ya nyumba yenye mpangilio."

Je, anaweka kila kitu kinapotakiwa, hata akivua nguo zake usiku haziachi kwenye sakafu? Je, anarundika vitu badala ya kupanga. Je kabati, pochi, begi la shule, lina mpangilio? Je, aweza kupanga mizigo yake vyema akienda likizo toka shuleni. Je, anavitupa tupa popote? Je, ana shida kupata vitu anapotafuta kama vile sindano, uzi, kazi ya shule au viatu vyake? Je, aweza kupanga mahali palipovurugika? Je, anaweza kutoa kipaumbele kipi aanze kufanya? Je, anapenda kukusanya vitu hata visivyo vya maana "junk" na hataki kuviachia? Je, anaweza kutunza miadi (appointments), anuani, na namba za simu bila kupoteza? Je, ni mtu wa mipangilio sana kichwani kiasi kwamba anapata hasira mipango ikibadilika? Je, unaweza ukamwachia nyumba ukaenda kwa siku moja? Je, anaandika mipango yake ya muda mrefu?

"Huangalia shamba, akalinunua, kwa mapato ya mikono yake hupanda mizabibu;" fungu la 16. Fungu hili laonyesha mipangilio ya kununua vitu, kupangilia kutunza mbegu na kupanga jinsi shamba litakavyokuwa kwa mfumo wa ufanisi na mazao bora. Hata kama ni mdogo, aweza kazi ndogo, kama -kuosha vyombo, kufua, kusafisha nyumba, kutunza wadogo zake, kwenda sokoni, kubadilisha nepi watoto. Kufanya kazi kutamsaidia kupanga mambo makubwa.

Wengi wanakazania shule, na hilo ni zuri, ila watoto wanasoma ili wapate kazi hatimaye. Kila anachofanya kina maana kwa Mfalme wa mbinguni kupata utukufu, na pia kinajenga tabia ambayo ndiyo pekee atakwenda nayo mbinguni. Tusidharau mianzo midogo, ndiyo inajenga watoto wetu kuwa wanawake hodari na shujaa. Msichana aanze kuweka magoli ya vikazi vya kufanya kabla ya kucheza. Mkatie kazi ndogo ndogo afanya na upange naye kadiri anavyozidi kukua.

Aweza kuanza kupanga magoli ya vitu vya kufanya vidogo vidogo hata vya ujasiliamali kama amefika miaka zaidi ya 14 hivi. Je, ana magoli gani ya kiroho siku za usoni kama kuonyesha upendo wa Mungu? Magoli ya mwanamke lazima yaendane na mume wake, jadilini kwa nini? Je, kuna kitu ambacho ni kigumu ambacho Mungu anataka ufanye katika maisha yako? Je, anapenda kumpendeza Mungu na kumpa utukufu na hilo ndiyo lengo lake kuangalia ya milele badala

ya ya muda? Je, malengo yake ya baadaye yanaendana na maandiko ya Mungu au ni ya anasa? Je, ana mipango ya anayotaka kufanya kila siku, na magoli ya baadaye, na anayaandika? Je, anaafikiana na malengo yenu ya familia na kuwaunga mkono kihali na mali? Je, yupo tayari kukosa raha za muda akilenga magoli yake? (mfano kusomea mitihani, badala ya kucheza). Je, ana shauku ya kujifunza mambo mapya, na kutumia ustani huu? Je, anajua Yesu anakuja na ni muhimu kujitayarisha kwa tukio hilo kubwa kupita yote?

Twaona bustani inasaida mambo mengi katika maisha ya mwanamke. Kwa kawaida inabariki anayelima na wengine pia. Bustani inaweza ikaleta uzuri, mazoezi, na hata mahali pa mtu kupumzika na kubarizi. Bustani si lazima iwe kubwa, nimeona wengi marafiki wa mjini wameweza kuweka maua au nyanya kwenye makopo, wakala mpaka wakagawa. Furaha ya kupanda mbegu na kuona zinakua ni muhimu. Kila msichana ajifunze kupanda mboga, na maua pia! Apate mafunzo ya kulima bustani kwa ufanisi, maana ni huduma nzuri kwa wale wenye mahitaji.

Wengi tulio na bustani tumetoa mazao kwa watu ambao ni wahitaji, na kubarikiwa. Ni vyema binti aandike insha ya faida za kuwa na bustani. Je, anajua tofauti ya magugu na mimea? Ukiwa unafanya kazi bustanini unafanya naye? Je, anajua kutayarisha udongo kwa ajli ya kupanda na jinsi na mahali pa kupata maarifa ya kilimo? Je, anajua jinsi ya kukabiliana na wadudu waharibuo mazao? Je ,anauliza ushauri kwa watu wengine maarifa ya kilimo? Je umempa kipande chake cha bustani alime? Je, anaweza kupangilia jinsi ya kuendesha bustani, na kufanya hivyo kwa msimu mmoja?

Mwanamke huyu wa mithali anapofanya mipango ya kununua na kulima, anakuwa ni mjasiliamali na mwenye kujua jinsi ya kupanga matumizi ya pesa vyema. Kwa vile mabinti zetu watakuwa wakubwa na kuwa na majukumu ya kutunza pesa zao, za waume zao na kusaidia watoto katika mipango mbali mbali; kumfundisha mipangilio ya fedha ni muhimu (financial training). Mtoto afundishwe kugawa pesa zake apewapo, kutoa fungu la kumi, na kuliweka kwenye bahasha au mahali tofauti. Kisha fungu la akiba, na fungu la matumizi. Ni vyema kusoma visa vya Marko 12: Mjane wa senti mbili; Mathayo 25 kwa mafundisho ya talanta na Luka 12 kuhusu tajiri aliyekuwa na mali nyingi.

Binti aulize watu mbali mbali, na hata wazazi kumsimulia mibaraka ya Mungu kwa wale waliorudisha zaka. Masomo ya tamaa ya pesa, kutumainia utajiri, kukopa na ubaradhifu wa pesa, ni muhimu. Mtoto afundishwe magoli ya fedha ya muda mfupi na muda mrefu. Je, atapataje pesa ya kununua kitu anachotaka? Wazazi wajadili, na kama kuna njia ya kumsaidia kufanya biashara ndogo ndogo, basi ni vyema kufanya hivi. Mtoto afundishwe kwamba kutoa ni bora kuliko kupokea, na Mungu hutubariki tunapotoa bila kunung'unika. Panapo nafasi mtoto afunguliwe akaunti.

Je, ni kanuni gani zitumike tunapokopa vitu? Je, aweza kulinganisha bei za vitu kabla ya kununua?Angalieni mifano ya Ibrahimu, Ayubu, Sulemani, Zakayo, Safira na Hezekia. Wekeni kumbukumbuku ya matumizi pamoja kwa mwezi. Fanyeni bajeti ya nguo kwa mwaka. Angalieni kanuni njema za kumkopesha mtu pesa. Awahoji wanawake wachache jinsi wanavyotunza pesa au kuweka akiba.

Je, kuna tofauti gani kati ya sadaka na zaka? Je, anatoa zaka na sadaka kwa ucheshi? Je, mke anawezaje kumsaidia mume wake kwa kuwa wakili mwema wa

mali? Unapofanya bajeti ya nyumbani mshirikishe aone matumizi ya nyumbani ya kila mwezi. Ni yapi tunayotumia pesa kila mara tunayoweza kuyakata au kupunguza? Je, kuna uzuri gani wa mke kukaa nyumbani au kuwa na kibarua nje ya nyumbani? Je, anajua kwamba yote aliyo nayo amepewa na Baba wa mbinguni? Je, ana shukurani kwa Mungu aliyempa?

Je, anajua kuweka akiba au anatumia pesa bila kufikiri? Je, ni bahili au yupo tayari kukirimia wengine kwa vile alivyobarikiwa na Mungu? Je, anatumia pesa kwa fujo? Je, anapenda kukopa kopa, au kutumia zaidi ya alivyo navyo? Je, anapenda kutumia pesa kwa anasa za muda badala ya kutunza? Je, anaweza kubajeti kutokana na pesa alizo nazo?

"Hujifunga nguvu viunoni kama mshipi; hutia mikono yake kwa nguvu;" Fungu la `17. Kama vile mwanajeshi aendavyo vitani kwenye Waefeso 6:17, anavyokuwa, ndivyo tunavyotakiwa na mabinti zetu. Ili mabinti zetu waelewe neno vizuri twapasa kujifunza nao kwa mfumo na mpangilio ili waelewe mafundisho makuu ya imani (doctrines).

Kila mtoto awe na biblia yake na akifika miaka saba hivi apaswa kuwa na muda wake wa kusoma Biblia, japo kwa dakika kumi. Pengine itakuwa vyema apate Biblia yenye lugha rahisi kwa kuanzia. Tumekuwa tukitumia Clear word Bible au International Children Bible.. Ila hatuna Biblia za watoto za Kiswahili. Kwa sasa tumeanza kuandika Biblia ya watoto au hadithi za Biblia za watoto, tuombeeni ili tuweze kumaliza kazi hii.

Hatuwezi kumjua au kumpenda Mungu bila kusoma Neno lake. Na Uzima wa Milele ni kumjua Mungu, kumtegemea, kumtumiani na kutembea Naye siku kwa siku; Yohana 17:3. Kuomba ni sisi tunazungumza na Mungu na kusoma Neno la Mungu, ni Mungu anazungumza na sisi.

Mama kama mzazi, lazima awe mfano. Je, watoto wanakuona unasoma Neno la Mungu kila siku? Mtoto aanze kuvikariri vitabu vya biblia 66 kwa mpangilio, au pengine kwa kutumia wimbo. Anakili vipande vya Neno la Mungu na kukariri. Kila siku mwaweza kusoma Mithali moja. Kusoma Neno la Mungu ni kitu cha kila siku, kama tunavyokula. Endapo tunaona tu busy sana, dawa ni kutokula chakula mpaka tumesoma Neno la Mungu. Tutajikuta tunasikia njaa na tutasoma. Mtoto anapojua kusoma tu, aanze kusoma Neno la Mungu. Muwe na chati ya kusoma kila siku, pengine kurasa moja, kwa siku au sura moja kwa siku.

Someni historia jinsi Neno la Mungu lilivyotufikia na mambo machache ya Biblia; mfano lugha iliyotumika, vitabu vya torati, historia, mashairi, zaburi. ilichapishwa mara ya kwanza 1456 na mashine ya Gutenberg, imebadilisha maisha ya wengi, iliandikiwa kwa miaka 1700 na watu kama 40. ina sura 1189 si kitabu cha mashauri bora au mawazo mazuri tu bali ni sauti ya Mungu na mamlaka ya mwisho duniani na mbinguni!

Binti asome Biblia na kuweka jina lake mfano 1 Kor 13. Pale penye Neno upendo aweke kwanza jina la Mungu kisha asome mara ya pili na kuweka jina lake. Kariri ujumbe (theme) muhimu katika kila kitabu cha Biblia. Mpeleke binti ahudhurie masomo ya Biblia kanisani (Bible study). Someni pamoja Zaburi 119 na jadilini. Angalieni njia mbali mbali za kusoma Biblia na kuomba neema ya kutenda yaliyoandikwa. Mwandikishe binti kwenye masomo ya Biblia ya Posta au ya online, kama amazingdiscovery.org, na amazingfacts.org, secretunsealed au

voiceofprophecy bible study. Akisoma fungu ni vyema aandike yafuatayo: Fungu hili linasema nini? Je, lina maana gani? Linawezaje kutumika maishani mwangu? Je, nifanyeje na hili fungu? Baada ya wiki aangalie kama kuna kilichobadilika kwa katika maisha yake kwa sababu ya lile fungu.

Je, anasoma Neno la Mungu kila siku bila kukumbushwa? Je, ana shauku ya kulisoma? Je, linabadilisha maisha yake na kuleta maana? Je, anaweza kutoa mifano, pale Neno la Mungu linaweza kutumika katika maisha yake? (application). Je, anauliza maswali akilisoma? Je, anashare na wengine? Je, anatafuta majibu kwa maswali yake kwenye Biblia? Je, anaweza akapata fungu kirahisi? Je, anajua angalau kwa mbali historia ya Biblia? Je, anajua jinsi ya kutumia mbinu za kusomea Biblia na kamusi zake, au Ufafanuzi wake, concordance na cross references?

Ni vyema mno kukariri Neno. Katika majaribu utamshinda mwovu kwa ahadi unazokumbuka tu! "Imeandikwa". Neno la Mungu tukiliweka moyoni kwetu ndiyo silaha kubwa ya kutotenda uovu; Zaburi 119:10. Roho wa Mungu atatukumbusha pahali pa kutoa upanga kwa jaribu Fulani. Aanze kukariri fungu moja kila wiki. Watoto wadogo wana kumbukumbu nzuri, na kwa vile hawana mengi kichwani, itasaidia. Hakuna jambo linaloleta akili kupanuka na kuwa na wingi wa maarifa kama kukariri Neno la Mungu. Jadilini anapoendelea kukariri ili aelewe maana ya mafungu haya. sura za kuanzia kukariri ni kama Zaburi 23, au 91. 1Kor 13; Amri kumi za Mungu au hata kitabu cha waefeso cha mahusiano, ni kizuri sana. Waweza kurekodi vile alivyokariri. Ni vyema kuwa na daftari la kuandika yale mnayosoma. Je, anaweza kukariri mafungu 20?

Kumfundisha binti mazoea ya kuomba kila siku ni muhimu, kwa vile hata atakapokuwa mtu mzima atajua kumletea Mungu shida zake, na katika shida atakazokuwa na familia yake itamsaidia kutatua matatizo kwa maombi. Daima tufundishe wote tunaowashauri kumpa Mungu shida zao. Ombeni pamoja asubuhi na jioni, aombe mwenyewe pia. Jadilini pamoja sala kuu ya Bwana katika Mathayo sita. Kila mara anapojaribiwa kumzungumzia mtu vibaya, aombe. Awe na daftari dogo la kuandika anayoombea na tarehe. Itamsaidia kurudi na kumshukuru Mungu. Aombee wenye shida, serikali, familia, shule, wazee, kanisa, waliokata tamaa, wagonjwa. Ajifunze kuombea wanaomuudhi. Kumsifu Mungu, kuungama dhambi, kumshukuru Mungu na kuleta haja zenu iwe sehemu ya kila ombi.

Awahoji watu wa imani, wamishonari au wahubiri jinsi maombi yalivyofungua njia, au jinsi Mungu alivyojibu maombi yao. Je, wanawake gani walienda kwa Kristo kumwomba jambo fulani? Andikeni ahadi za Mungu na jinsi ya kuziomba? (zipo zaidi ya 3500). Aanze kuombea mume atakayemwoa japo ana miaka kumi na, tu.

Asome visa vya imani kama cha Hana, Musa, Sulemani, Nehemia au Daudi. Someni maisha ya Agustine, John Newton na wengine wanaoshukuru maombi ya mama Zao yaliyoleta tofauti katika maisha yao. Jifunzeni kanuni za maombi ya kufunga jinsi binti anavyokua. Je, anafumba macho akiomba? Je, maombi ni kitu halisi kwake, yaani mawasiliano halisi na Mungu au ni mapokeo tu? Je, anaomba uongozi wa Mungu kabla ya kufanya maamuzi? Je, anafikiri kuomba akiwa na shida? Je, anaonyesha kicho kwenye maombi, au anazungumza na kuchezacheza? Je, anaamini Mungu anajibu maombi? Je, unamwambia maombi

yako yaliyojibiwa kupitia kwake? Je, anatoa shukurani kwenye maombi yake, au anaomba vitu wakati wote?

Ni vyema kuwafundisha mabinti zetu kutawala nafsi. Kukabili miili yao au hisia zao. Ni muhimu sana kujikana nafasi, kwenda kulala kwa wakati na kuamka kwa wakati. Kusoma Neno na kuomba mara baada ya kuamka. Kula kwa wakati na kujifunza kanuni nzuri za kutunza mwili (kupiga mswaki, kuchana nywele, kukata kucha, kuoga, kufua nguo) bila kukumbushwa.

Ajifunze kula akiwa na njaa, si kwa sababu hana kitu cha kufanya hivyo chakula kinakuwa rafiki. Asile mlo mpaka masaa manne au matano yapite. Uvivu, ulafi, kuvaa nguo zisizo na heshima, maisha ya uovu, marafiki wabaya ni mambo ya kuyakana.

Je, anasikiliza muziki wa aina gani? Aulize wengine wamwambie vitabia alivyo navyo ambavyo vinawachukiza wengine ili aviache kwa neema ya Mungu. Je, anajua chakula cha afya na kufanya mazoezi, au anakula chochote bora anakifurahia? Je, anajua Neno la Mungu lataka tuleje?

Asome maisha ya watu waliojikana nafsi ili kufanya mambo makuu katika maisha, mfano Daniel, Esta, Yusufu. Aandike insha ya 'Ulafi'.

Mkae mahali barabarani watu wanapopita muangalie watu. Je, wanavyotembea, macho yao, nguo zao au mtembeo wao unaleta mawasiliano fulani? Je, yupi atakuwa anajiamini, anajikana nafsi, au mvivu? Neno la Mungu linaitaje miili yetu? Soma hasara za kula mno au kula kidogo? Soma hasara za kula chakula kisicho na afya (junk food) au kile Mungu anasema tusile.

Kuna dhambi zinaathiri miili yetu kama vile hasira na zinginezo, zichambueni hizi. Soma sheria za afya na ulaji kwenye agano la kale kama toka wakati wa Nuhu kabla ya wayahudi. Angalia kama anajitahidi kuishi maisha ya afya,na usafi bila kukumbushwa, anapiga mswaki? Anafua nguo zake za ndani kila siku? Anaoga kila siku bila kukumbushwa? Je, anafanya mazoezi, na kujikana nafsi katika ulaji wake? Je, anajua kwamba mwili wake ni hekalu la Roho Mtakatifu?

Je, mwonekano wake unaonyesha kujikana nafsi na kujiheshimu? Je, anatawala mwili wake ili asiwakere wengine? Je mara zote anaonekana amechoka? Je, mara nyingi ni mgonjwa? Je, anakaa kwa adabu? Je, kuna mambo ya kumsaidia ili awe na afya na nguvu? Je, anatabia za wasiwasi (nervous) kama vile kula kucha zake? Je, anajali anavyoonekana kwa watu? Je, anajali kupita kiasi mwonekano wake kwa watu?

Ni muhimu kuwafundisha mabinti zetu kupata ushauri unaofaa. Mungu ndiye mshauri mkubwa, ila ameweka watu pia watusaidie. Aweza kuwauliza wanawake watu wazima wacha Mungu. Atakapokuwa mtu mzima mara kadhaa atahitaji mashauri ya watu. Ni vyema kuwa wanyenyekevu kuuliza ushauri kuliko kuharibu mambo pale tunapokwama. Neno la Mungu katika Yakobo moja, lasema yoyote kati yetu asiye na hekima aulize, na Mungu atampa. Awaulize wazazi mahali ambapo katika maisha yenu mmeomba ushauri na kufanikiwa.

Kitabu cha Mithali ni kizuri kukisoma na kila mara asema "Mwanangu sikiliza mausia yangu….". Je, atafutaje mshauri bora wa mambo ya kiroho, mambo ya nyumba, mambo ya jamii au mambo ya fedha? Tito 2 yasema wanawake wazee wawe washauri. Soma watu waliopokea ushauri mbaya au mzuri kwenye Neno Mungu.

Je, Hekima ni nini? Someni Efeso 5 :22-24 na kujadiliana: Kumtii mume

kuna maana gani katika kupata ushauri wa wengine? Je, mke afanyeje mume wake anapompa ushauri usio na hekima kama Abigaili?

Nakumbuka ushauri alionipa mama yangu kabla ya kumaliza darasa la 12 alipoona watu wanakuja kuulizia posa au uchumba. Hata niliposoma kwenye seminari kwa vile nilikuwa msichana peke yangu, na hata chuoni kwenye kitivo cha kemia nilikuwa ni msichana pekee. Na huu ulikuwa ni umri wa watu kutafuta wasichana wa kuoa. Wavulana waliokuja mama alinishauri: "Unaona watu wanavyokuja wengi sasa angalia usiwe na majibu ya dharau au jeuri, hata kama sasa unasoma na hutaki kuolewa, wajibu vizuri na kwa heshima, hata wale unaofikiri hawastahili kwa vile wana tabia mbovu. Waambie wakupe muda kufikiria jambo hili, na baada ya siku chache waambie kwamba upo shuleni bado, au una mambo fulani ya kukamilisha hivyo waendelee tu kwani haitawezekana." Akasema pengine baada ya miaka michache utakuwa umebadili mawazo, na kwa vile ulikuwa umewajibu kwa wema tu wanaweza kurudi na ukapata mtu mzuri wa kukuoa. Na hata isipokuwa wao, watakuzungumza vizuri kwa watu, na wale watu wataamini unajali watu.

Dunia inabadilika, leo wanataka kuoa, wewe hauko tayari, kesho utataka kuolewa nao watakuwa hawako tayari kwa sababu ya dharau au majibu yako. Kisha akasema si kazi ya msichana kumkimbiza mwanaume kama mke wa Potifa, wanaume wakufuate wewe, wale wanaokufuata ndio unamchagua mmoja kati ya hao. Ni aibu kumfuata fuata mwanamume, hata ukiwa unampenda, mwache akufuate. ingawa siku hizi wasichana ndo wanakazana sana kutafuta!'. Mwanaume aliumbwa ili atafute, na anajisikia vizuri akiona amempata, msichana au ametia bidii. Zaidi ya yote, kuombea kupata mume bora hata zaidi ya mara tatu kwa siku ni muhimu maana hakuna ajuaye anayefaa. Wale walionekana wa kihasara, wamekuwa waume bora, na wale walioonekana wema, wamekuwa makatili kwa wake zao, moyo ni mdanganyifu, una magonjwa ya kuficha, ni nani aujuaye isipokuwa Mungu tu? Basi msichana ajue mume bora ni Bwana anayetoa, na si yeye kwa maarifa yake atampata.

Watu hubadilika, wale walioolewa na watu wa kufaa au 'stable,' wale watu walibadilika wakawa wabaya kwa wake zao, na wale tulifikiri walipata watu wasiofaa, wamebadilika. Mwenzi wa mtu aweza kufanya tabia yake ibadilike kwa kumpa nafasi ya kukua. Angalia zaidi kwenye Biblia wazazi walipotoa ushauri.

Je, binti anakufuata umpe ushauri kwenye mambo ya kawaida na nyeti? Je, anakubali ushauri wako kuhusu marafiki zake au anabishana? Je, anafikiri mara zote yupo sawa? Je, anaomba ushauri wa mambo ya kiroho? Je, anatafuta kujua mapenzi ya Mungu kwa kusoma Neno lake? Je, anafurahia mashauri ya Mungu na wale wanaompenda Mungu, au anataka njia zake tu?

Kwa vile tuko katika jumuiya ya waumini, ni vyema tutiane nguvu na wale ambao tunaamini sawa. Tuwahusishe mabinti zetu na kanisa na kujadili mahuribi, na Neno la Mungu pamoja. Mabinti zetu waone thamani ya kusaidia shughuli za kanisa. Waweze kusaidiana na shemashi kusafisha kanisa. Wawashukuru walimu wao wanaowafundisha kanisani na viongozi. Kuna huduma nyingi kanisani, za kusaidia wenye mahitaji; mabinti zetu waweza kujumuika

Mabinti zetu wajifunze jinsi ya kukaa kwa utulivu kanisani na kutunza siku ya Bwana kwa mpango wa Biblia ulioagizwa. Je, wanawake wa Agano la kale na jipya walikuwa na sehemu gani katika kanisa?

Je, analalamika kwenda kanisani na kuepuka? Je, anatokatoka kanisani kwenda chooni au kunywa maji kila mara? Je anatumia yaliyofundishwa kanisani? Je anaomba akila tu, bali haombei maisha yake ? Je, marafiki zake wa karibu ni wa kanisani? Je, anafurahia kuwa katika nyumba ya Bwana? Je, anaweza kusema alichofundishwa leo? Je, anahudumia wengine na talanta alizopewa? Je, anasikiliza kwa makini? Je, anaombea mahitaji ya mwili wa Kristo? Je anajua karama zake za Roho? Je, anawapenda (admire) wanawake wa kanisa lake au viongozi au anawapenda watu wa dunia (celebrity)?

"Huona kama bidhaa yake ina faida; taa yake haizimiki usiku;" fungu la 18 . Mwanamke wa huyu ni mvumilivu, (perseverance). Kama wazazi tuepuke majaribu ya kuwakinga watoto wetu wasipate shida au mambo magumu. Watoto wasipate kuona toka kwetu kwamba Mungu anawatendea visivyo haki. Tuwasaidie wamrudie Mungu na Neno lake. Tusiwapunje watoto wetu nafasi ya kuona ukuu na uaminifu wa Mungu katika shida zao ili wakue na kusafishwa kuwa vito safi. Vitabu kama Pilgrims progress ni vizuri kuona hili. Wawaulize wazee wa imani uaminifu wa Mungu katika maisha yao. Waebrania 11 ni sura ya kusoma na kujadili watu hawa jinsi walivyotatua shida zao wakisaidiwa na Mungu. Tunapokuwa na wakati mgumu, ni nini kibaya kitatokea? Ni nani anashika hatamu za mambo yote? Kutii na kuamini kunasaidaje kuwajulisha wengine kwamba Mungu ndiye Mweza.

Soma maisha ya watu mashuhuri ambao hawakukata tamaa wakati wa dhiki kuu au kufeli. Someni zaburi, na magazeti kama 'Voice of matyr' kwenye kompyuta ya watu waliokufa kwaajili ya imani siku za karibuni. Someni Isaya 53. Je, ni watu gani kwenye Biblia walistahimili mpaka mwisho? Je tunawezaje kushukuru kwa kila jambo? Jadilini ukuu na uwezo wa Mungu pamoja. Je kwanini Mungu anaruhusu majaribu na mateso? (1Petro). Je, ni kwa jinsi gani mke anaweza kuwa mvumilivu na mtiifu kwa mume ambaye ni mgumu kuishi naye? Je, Biblia inasemaje kuhusu talaka? Talaka na uvumilivu zinahusianaje?

Je, anakata tamaa haraka na hataki kujaribu tena kama alishindwa? Je, analalamika na kujihurumia kama mambo hayaendi anavyotaka au mtu amemkosea? Je, anaweka akili yake kwenye matatizo tu? Je, anaweza kutalawa hisia zake wakati wa shida au akiwa ana matatizo bila kuwa na chuki? Je, anajionyesha kwamba ni yeye tu mwenye matatizo duniani? Je, anapata faraja ya maandiko akijaribiwa au akiwa na shida? Je, anajihoji kwa dhambi zake akiwa na shida, ili aone pengine Bwana ataka kumrudi? Je, anajua kwamba Mungu anataka ajifunze katika shida zake? Je, anampa utukufu Mungu kwa jinsi anavyokabiliana na shida? Je, anamtumaini Mungu, na kuona majaribu yanamsaidia akomae?

"Hutia mikono yake katika kusokokota. Na mikono yake huishika pia. Huwakunjulia masikini mikono yake; naam huwanyoshea wahitaji mikono yake;" fungu la 19-20. Mungu ametukarimu na anatualika nasi tukarimu wale tusiwaowajua, na kuonyesha upendo kwao. Mwanamke anajifunza ukarimu kwao, anapokuwa mdogo. Nyumba inayokaribisha wale wanaohitaji faraja, ushirika, msaada, na upendo ni nyumba ya mfano bora. Mama ataleta hali ya furaha katika kushiriki kusaidia wengine. Wengi twaambiwa wamekaribisha malaika bila kujua (Waebrania 13).

Tufundishe watoto kuwa wakarimu, kwa kupeleka chakula kwa wagonjwa, kusaidia wenye mahitaji kama wazee na wagonjwa, kualika watu nyumbani

mwetu. Wafundishe watoto jinsi ya kumsalimu mgeni akija, kumtambulisha, kupokea mizigo yake, kuzungumza naye, kumhudumia chakula, na kumfanya ajisikie huru (ease). Jadilini, yeye kama mwenyeji afanye nini? Je, awezaje kusaidia familia kwa mgeni asiyetegemewa? Je, awezaje kusaidia watoto wa mgeni waliokuja kuwatembea na mama yao? Fikiria mtu ambaye mkienda kwake anawakaribisha kwa furaha na jaribu kumwiga.

Je, wageni wanaokuja kanisani awezaje kuwakaribisha wasikie wamependwa? Someni mifano ya waliokaribisha wageni kwenye Neno la Mungu. Je ni nani alikaribisha malaika? Angalia mifano ya Martha na Mary kwenye Luka 10 na Yohana 12. Je, anaweza kupika chakula rahisi kwa upesi na kuwapa wageni? Je, anajua chakula wanachopenda watoto? Kwa wageni wanaolala, aweza kusaidia? Je, kuna tofauti gani kati ya mke na mume kwenye kukaribisha wageni? Je, anakaa na wageni au anajitenga

Je, yupo tayari wageni watumie vitu vyake? Je, anaingilia mazungumzo ya watu wazima kwa adabu? Je, anajitahidi kuanzisha mazungumzo na mgeni? Je anajaribu kuwa mkarimu kwa wageni hata wasio wa umri wake. Je, anasaidia wageni wajisikie wapo 'nyumbani"? Je, marafiki zake wakija anachukua jukumu la kuwakaribisha na kuwahudumia? Je!, ana adabu akikaa kwenye meza kuzungumza na wageni? Je, anawakirimu wageni wa kanisani na kuwasalimia? Je, anachukia wageni wakija kwa vile atakuwa na kazi nyingi? Je, anajua kwamba ukarimu wake ni jinsi ya kumhudumia Mungu? Je, anaona nyumba yao ni gurudumu la kufikia watu wamjue Mungu?

Kwa upande mwingine ajue jinsi ya kuwa mgeni bora, anapotembelea wengine. ucheshi, na kuwa na adabu pale alipo. Kuvaa nguo kwa heshima, hata kama ni wakati wa kwenda kulala. Jinsi ya kujibu watu au kufanya mambo kwa hekima. Mfano akisikia wenyeji wake wanagombana afanyeje? Shughuli gani aweza kumsaidia mwenyeji wake

Kuwa mwanamke mwenye rehema ni muhimu. Kusaidia masikini, kutia watu matumaini kiroho na kimwilli ni muhimu. Amhurumiaye Masikini, humkopesha Bwana, na Bwana hulipa bila kupunja. Watoto wa Mungu si mabahili bali hutoa. Mfundishe kutoa vitu vyake vya michezo, nguo zake n.k.

Pangeni jinsi ya kusaidia wajane, wagonjwa, vilema, wapweke, yatima, au wazee kanisani mwenu. Jinsi ya kuweka kando pesa za kusaidia wenye mahitaji; mfano walio jela, wamishonari, wanaotunza wagonjwa, wajawazito, watu wenye maradhi ya akili, watu waliodhulumiwa n.k. Je, mnaweza kuwasaidiaje? Je mafungu gani ya Neno la Mungu yatakuwa faraja kwao? Angalia www.persecution.com.

Soma vitabu vya injili na angalia jinsi Kristo alivyosaidia wenye mahitaji. Alisaidiaje masikini, wagonjwa, wajane au yatima. Soma gazeti au sikiliza taarifa ya habari na kuona mtasaidiaje waliopata maafa. Je, waweza kusaidia majirani zako ambao ni masikini bali hawatakiwi kupewa vitu bali ajira? Huruma au rehema in maana gani?

Je anaona watu wanapoteseka, au wanapokuwa na mahitaji? Je, ana huruma na mahitaji yao? Je, anapata huzuni na kuonyesha rehema kwa wahitaji? Je, anajua kusema maneno ya faraja kwa wale wenye maumivu? Je, anatoa muda na mali yake kwa kumpenda Mungu au atoa ili watu wamwone? Je, ana shauku ya kumfuata Kristo kwa kuhudumia watu? Je, anafurahi kuhudumu? Je, anajitoa

kwenye huduma za kujitolea?

Twapasa kuhusika kwenye kusaidia mahitaji ya watu ya kiroho pia. Kama wanawake twahusika na haya kila siku. Tumeamriwa kwenda dunia yote na kuwaambia watu habari njema. Ni vyema aelewe kwa ufupi jinsi ya kutoa ushuhuda. Je, alikuwaje mkristo; ? Mungu amebadilishaje maisha yake. Ajue kisa cha msalaba hata kwa ufupi; kwamba wote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu Warumi 3:23 na 6:23. Mshahara wa dhambi ni mauti, tunaokolewa kwa neema tu. Mungu anatupa neema tukiamini; ni lazima tuungame dhambi zetu na kuwa na toba ya kweli, tumwamini Kirsto kama Mwokozi wetu na tuna uhakika na Wokovu.

Je, aweza kumsimulia rafiki wokovu maana yake nini? Je, aweza kuomba na mtu na kumsaidia kuomba toba ya kwel? Aweza kuwa na klabu ya Biblia kwa watoto wa jirani? Watu walisaidia mahitaji ya kimwili ili kumsaidia mtu kiroho. Je, aweza kuchangisha pesa kwa mradiya kusaidia mahitaji ya kanisa, kama ujenzi?

Je, anaamini kuwa Yesu alikufa na kufufuka ili alipie dhambi zake? Je, amemkubali Kristo kuwa Mwokozi na Bwana wake? Je, anaumia kwa wale wanaopotea bila kumjua Mungu? Je, anawaombea wasiomjua Mungu? Je, anajua mafungu ya kumwongoza mtu kumwamini Mungu? Je, anaona aibu kumkiri Kriso kwa wengine? Je, anapenda kumtii Mungu? Je, maisha yake yaendana na Neno? Je, anaombea watenda kazi wanaomtumikia Mungu na kuwatia moyo? Je, anatoa alichonacho kusapoti kazi ya Mungu au anafikiria maisha hapa hapa tu?

Kuwa mtu wa haki ni moja wapo ya tabia ya mwanamke bora. Ni vyema ajue mambo yahusuyo sheria za nchi. Kupiga kura na kuheshimu viongozi. Ajue viongozi wanawekwa na Mungu na ni muhimu watende haki. Je, amchague nani anapopiga kura? Kuna ajenda nyingi mkristo anazopaswa kufikiria: Kama kutoa mimba, kuua wagonjwa (euthanasia), kuhukumu kunyonga, ushoga, ponografia, kutoza kodi, uasherati au uongo. Je, mtu anayempenda Mungu ahusikaje na hizi? Je, anapopiga kura ampigie kura viongozi anayeunga mkono haya? Je, kuna viongozi wanaompenda Mungu walioleta baraka kwa watu? Soma maisha ya Daniel, Nuhu, au Rehoboamu.

Je anajua viongozi wake, na anajua mamlaka yana maana gani? Je, anaweza kutoa hoja yake kupeleka kwenye uongozi wa ngazi za chini na hata juu? Je, anajua jinsi mswaada unavyokuwa sheria? Anajua mambo yanayoendelea nchini sasa hivi? Je, anaweza kugundua maneno ya yanayoposha ya "mawazo ya binadamu" kwenye vyombo vya habari? Je, anaonyesha heshima inayoakiwa kwa viongozi wa serikali, hata wale wenye ubinafi na uovu? Je, pale alipo anajitahidi kubadili sheria mbovu kwa kuzungumza na viongozi mahalia? Je, anahudumia majeruhi waliokosewa haki? Je, anajua kwamba mamlaka youte imewekwa na Mungu?

" Hawahofii theluji watu wa nyumbani mwake, maana wote wa nyumbani mwake huvikwa nguo nyekundu;" fungu la 21.

Mwanamke hodari hujihami na wakati ujao. Ni vyema binti ajue simu za kupiga za dharura, kama vile ndugu wa kuomba msaada, polisi au zima moto. Yusufu alitayarisha Misri kwa wakati wa shida (Mwanzo 41). Nasi pia tuwafundishe watoto wetu kufanya hivyo. Tuwafundishe kujua cha kufanya moto ukianza kutokea, pa kukimbia na jinsi ya kusaidia wadogo zao. Ajue tochi, vibiriti au mishumaa vilipo.

Ukimwachia alee watoto wadogo, mfundshe vizuri jinsi ya kuwachunga na hatari zinazoweza kutokea na anavyoweza kuzikabili. Je, kuna majani au maua ya sumu karibu? Je, mtoto akinywa mafuta ya taa au akizama kwenye mto afanyeje? Mhoji mama ambaye amekutana na matatizo ya hatari za watoto nyumbani, alifanyeje? Mfundishe binti hatari za maji, umeme na gesi, na jinsi ya kuzima inavyotakikana.

Huduma ya kwanza ni muhimu; kila mtoto afundishwe kwa uwezo wa umri. Je, mtoto akiugua ghafla anajua cha kufanya, na mtu wa kumwuliza na kisha ampeleke mtoto hospitali? Je, sehemu mnayoishi ina hatari za aina gani, ni yapi mfanye mkiishi hapa? Je, anaweza kujua chakula kimeharibika na cha kutupa kisije kikasumisha watu? Je, mabaki ya chakula ni ya kutupa? Je, nyama, Mayai au samaki zinatunzwaje?

Je, mshikio wa sufuria hugeukia upande gani?, unapompa mtu kisu ushike upande gani? Je, anajua jinsi ya kutumia presha cooker kwa usalama? Mfundishe jinsi ya kutunza mboga kwa usalama, kwa kukausha au kuweka kwenye chupa. Ajifunze machache ya usalama kwa vyombo vya usafiri kama vile baiskeli, pikipiki au gari. Je, aweza kubadilisha matairi? Je, anajua jinsi ya kupata chanjo bila kudhurika? Mfanye utafiti wa pande zote.

Kitabu kama “Mahali pasipo na Daktari” ni kizuri, kuwa nacho. Ni wakati gani huduma ya kwanza ya nyumbani haisaidii na lazima mtu apelekwe hospitalli? Jifunze na binti tiba mbadala na kukuza mimea ya tiba (herbs for medicine kama vile echinecia, tangawizi, vitunguu saumu). Chukueni madarasa ya kuokoa mtu majini, kujilinda (self defence class). Jifunzeni usalama wa kuwa/kutokuwa na silaha mbali mbali nyumbani, kama mishale, rungu, mitego ya panya au sumu za panya au bunduki.

Je, anajua wakati wa tahadhari kama haupo? Je, anajua kuogelea? Je, anaweza kuwa na upeo wa kuona hatari inayokuja? Je, anakuwa mwangalifu ili asiwe hatari au kuumiza wengine? Mfano kuacha maji bila kudeki, kurusha vitu, n.k. Je, akiharibikiwa na chombo cha usafiri anaweza akawa msaada? Je, anajua jinsi ya kukabiliana na dharura ya nyumbani? Je, anashughulika na chakula kwa usafi na usalama? Je, anajua cha kufanya endapo tetemeko, au dhoruba ikitokea? Anaweza akatumia vyombo vya kazi kwa usalama? Je, anajua kujikinga na maradhi? Je, anajua kujikinga na mtu anayetaka kumpiga? (self defence moves), Je, anamtumaini Mungu kama kinga yake kuu na mpaji?

“Hujifanyia mazulia ya urembo, mavazi yake ni kitani safi na urujuani” fungu la 22.

Mwanamke anayemcha Mungu anapenda vitu vya kupendeza pia, anajitahidi ashone na kujua ustadi fulani. Anajitahidi katika kuvaa vizuri hata nyumbani, asiwe kama yule anayekimbiza ndege shambani, avaaye vizuri akitoka nje ya nyumba. Ajifunze kutandika kitanda chake na kuacha chumba chake katika hali nzuri akiamka. Chumba kinabadilika kabisa, kwa kutandika tu kitanda! Aweza kusaidia kufuma vitambaa vya viti na meza. Kupanda maua na kuweka nyumbani, kusaidia ndugu zake kushona vifungo. Mungu ametuumba tupende ustadi na nakshi. Mfundishe kushona, kukarabati nguo , kama huwezi mtafute mtu amsaidie. Ajifunze kuweka zipu, kushona begi, kushona kitambaa cha mkononi, nguo ya mtoto, sketi, apron. Mwaweza hata kushona na kusaidia wenye mahitaji. Kuhudhuria madarasa ya ushonaji, upambaji, ufumaji kupata maarifa zaidi.

Kina mama waweza kufundisha haya kwa wasichana kwenye nyumba za ibada au jumuiya. Vitabu kama “Simple secrets to a beautiful Home;” by Emilie. Barnes, ni vyema kuwapa wasichana wetu wavisoma

Je, chumba chake kina mpangilio? Je, anajaribu kukifanya chumba chake kuwa safi na maridadi? Je, meza, viti , nguo na matandiko yake yamekaa sawa? Je, anachukua muda kujifunza kupamba, kwa maua na vitu rahisi chumba, nyumba au hata kushirikiana na wengine kulipamba kanisa la Mungu? Je, mapambo yake ya kuta ni ya picha za watu wa dunia na celebrity na magazeti ya watu wa anasa, au ni mambo ya kumsaidia?

Yaonekana mwanamke huyu anavaa kitani na zambarau, hizi ni nguo za kifalme, ni binti wa mfalme huyu! Nafikiri kama tuna uwezo tuwe na nguo chache nzuri, na pia kusaidia wenye mahitaji. Kuwa mtoto wa mfalme ni pamoja na tabia ya kifalme. Mabinti zetu wajifunze tabia za adabu na upole za kifalme. Kusema asante, tafadhali, samahani, pole ni maneno ya dhahabu au kifalme. Wajue jinsi ya kuwa watulivu kanisani na kwingineko; na si kupayuka payuka na kuongea kwa sauti ya juu, au kubishana. Wajue jinsi ya kumwita mtu au kuzungumza na mtu. Wajue sheria (rules) wanapotembelea watu wengine. Gary na Cathy Maldaner wameandika kitabu “Visiting other families in polite moments”. Jaribu kuona ni mambo gani ya kufundisha watoto wajue mnapotembelea mtu (ugenini).
Je, mnapoenda kwenye hoteli au mgahawa mfanyeje, (adabu na kujistahi-polite manners). Jinsi ya kuserve chakula, jinsi ya kuomba menu, kutumia kijiko au uma, au napkin (karatasi ya kujifuta mdomo). Andikeni sheria hizi mahali na kujifunza pamoja. Mfano ni nani anaanza kuserve chakula mkiwa wageni mahali? Vitabu kama Manners made easy by June Hines Moore ni msaada.

Jinsi ya kujibu simu, na kujitambulisha unapokutana na watu. Jinsi ya kumsifia mtu au kumtia moyo (compliment/praise), jinsi ya kumlaki mgeni mlangoni mwako, jinsi ya kushukuru ukisifiwa, jinsi ya kushukuru ukimaliza ukaribisho, jinsi ya kupenga makamasi, kupiga chafya au kukohoa mbele ya watu. Jinsi ya kutoa hudhuru ukienda chooni, jinsi ya kupanga meza na kupakua watu wale, jinsi ya kufanya mtu akusikilize anayefanya kazi Fulani (interrupting). Jinsi ya kuwa mgeni bora ukialikwa mahali, jinsi ya kutokuwa mchoyo na kutojifikiria, au jinsi ya kuandika shukurani kwa waliokualika ukirudi.

Je, msichana ajifunzeje jinsi ya kufanya mambo kwa tanashati (a girls guide to etiquette) Someni vitabu vya injili, Je, unajifunza nini kuhusu Kristo kama mgeni, rafiki, mwalimu. Aliwasalimuje watu, alizungumzaje nao, aliaganaje nao, Soma jinsi Nabali 1Sam 25 na Hanuni 2 Sam 10; walivyokuwa na adabu mbaya. Je, wafilipi 2:2-4 inatusaidiaje kuhusu mahusiano na watu?

Andika list ya vile vitu vinavyowasinya watu (annoy) au ambavyo havionyeshi tabia njema (bad manners). Andika jinsi binti anaweza akabadili tabia hizi mbovu. Andika watu ambao ungependa kuwa nao, angalia tabia zao, Je, wana tabia gani za kiungwana (polite habits)? Je, wanaheshimu wengine kuliko wenyewe, linganisha na tabia yako. Angalia mfano wa mwanamke mwenye tabia njema muulize anafanyaje haya (graciousness and good manners/etiquette). Je, tunda la roho linahusikaje na tabia zetu Gal 5:22-23.

Alika mgeni kisha panga binti apange meza, aweke maua , apike na kuwa mwenyeji ( gracious hostess). Angalia kwenye Neno la Mungu wale walioonyesha tabia njema, walifanya nini? Je, wapi biblia yatuambia tuwe na upole na utu

wema (politeness/kindness); kama kujali wazee au kuhudumu wengine kabla yetu. Je, kwa nini si vizuri kuzungumza ukitafuna chakula mdomoni?

Je, anawafanyia wengine vile anavyopenda kufanyiwa? Je, ana tabia njema akiwa mezani (manners), Je, anazungumza kwa kujali watu (politely)? Je, anajua kutoa udhuru anapotakiwa, Je, anapenda watu na ana tabia njema ( good etiquette) akifuata sheria zake kwa unyenyekevu na upendo kwa wengine. Je, wengine wapenda kuwa kuzungumza naye au kumtembelea? Je, mara nyingi unapata aibu ukiwa na wageni wako kwa tabia au jinsi anavyozungumza na watu? Je, anaonyesha adabu kwa wazee? Je, anajua kutoa shukurani, na anaheshimu vitu vya watu?

Ni vyema kuwafundisha watoto kuwa na kiasi. Tuwafundishe kwamba wanavyovaa au kuzungumza waweza kukwaza watu. Tuwaambie jukumu lao kuwa na hekima katika kuvaa, na kuzungumza na watu. Lazima wajue wao ni watoto wa Mfalme, na kufundishwa tangia wakiwa wadogo. Tuwavalishe kwa style zinazofaa toka udogoni.

Mara nyingi watoto wa kike wadogo wanavalishwa nguo za wazi, kama vikaputura vifupi, na mtoto akifika miaka 12 tunaanza kumwambia hiyo haifai na ameivaa toka udogo! Watoto wadogo ni vizuri wavalishwe kaptura wakiwa na magauni, maana wakicheza nguo za ndani (chupi) zaonekana. Mtoto asitembee amefunga kanga iliyoacha mabega siku nzima, bali aongeze na nyingine ya kufunika mabega/kifua.

Tuwafundishe pia kuwa wanyenyekevu wenye kiasi, na wasiojisikia kwamba wao ndiyo muhimu kuliko wengine. 1Tim 2, yaeleza mwanamke anayempenda Mungu. Je,mavazi gani au fashion ambazo hazina kiasi? Lazima kuwe na jinsi ya kuvaa (dress code). Je, wanavaa suruali (trousers) za aina gani? Je, zinabana hasa kwenye sehemu za siri? Je, nguo zinaonyesha kifua na matiti? Je, magauni yako juu ya magoti? Mwambie binti azungumze na baba yake kuhusu nguo ambazo hazileti majaribu kwa vijana wa kiume au hata wanaume watu wazima.

Chukueni Catalog ya nguo za wanawakezenye picha na kuijadili. Kaeni mahali na kuona watu wanaopita na kujadili nguo ipi ni ya kiasi na ipi haina adabu (immodest). Je, unapima nguo hizi kutokana na kiwango gani? Andikeni sheria ya nguo za msichana anayemwakilisha Mungu, na jinsi ya kutengeneza nywele, kucha au uso kwa kumwakilisha Mungu. Je, mwonekano wa nje unajalisha au bora mioyo yetu ni safi hivyo inatosha? Ni kwa nini Mungu alitupa nguo bustanini mwa Edeni? Kwa nini hakuwaachia wakae na majani yale ya mikuyu waliojitengenezea yaliyowafunika kidogo tu na kuacha utupu mwingine? Kama Mungu alitupa nguo, ya kufunika mwili na si majani, hii ina maana gani kwetu?

Angalia fasheni ya nguo ya nchi mbali mbali, kisha angalieni miaka 50 hata mia ya nyuma watu walivyovaa. Je, hizi fasheni zinawakilisha maadili na utamaduni wa watu hao? Binti ajadili na wazazi kwamba goli lake ni lipi katika uvaaji wake? Anavaa kumpendeza Mungu au wanadamu; na anataka watu wamwone au amletee Mungu utukufu?

Nchi nyingi siku hizi wana sehemu ambazo familia yote inaenda bila nguo kabisa (nude beaches, or recreation); kwa nini hili ni kosa? Kwa nini Nuhu alimlaani mwana wake aliyemwona uchi? Wakati Kristo yupo duniani watu walivaaje? Je, uchi ni nini?Je! Ni kutokuwa na nguo kabisa au kuvaa nusu nusu, sehemu zingine zikiwa wazi?.

Neno la Mungu liko wazi kuhusu sehemu za mwili za kuacha wazi na za kufunika. Mwambie binti aende na baba yake kununua nguo zake, na baba atoe mawazo kwenye uchaguzi, kisha aseme kwa nini amechagua nguo hiyo. Mwambie baba yake naye waangalie nguo zake kabatini na wazithathmini na kutoa sababu kwanini zinafaa au hazifai.

Soma mwanamke mgeni kama wa Mithali saba. Je, anafanya nini kuwavuta wanaume? Linganisha wanawake wawili wa ufunuo, yule aliyevikwa jua na mwezi na yule aliyedanganya mataifa. Tofauti yao ni nini? Wanaume wa namna gani waenda kwa wanawake wageni? Mwulize baba amweleze binti jinsi vijana wa kiume wanavyoona mwanamke akiwa na nguo imebana, au inaacha sehemu nyeti za mwili, anafanya watu wampe umakini usiofaa (flirtatious). Someni kitabu "For Young women only" kilichoandikwa na Shaunti Feldhahn na jadilini wote nyumbani mwenu.

Someni Mathayo 5:27-28. binti anapovaa afikiri kuhusu wanaume watakaomwangalia na yale watakayofikiri. Fikiria mwanamke mwenye adabu na roho ya kicho (modesty in spirit and dress).Angalia tabia yake, matendo, na jinsi anavyozungumza na wanaume, au anavyovaa. Soma wanawake wasio na kicho na jinsi walivyovaa. Walifanya nini?, matokeo yake yalikuwaje? Je, kutovaa vizuri kwawezaje kuwa kukosa uaminifu kwa yule utakayeolewa naye? Je, inasaidiaje wavulana wengine kukosa uaminifu kwa wake zao watakaoa? Mtayarishe binti kwa uchumba atakapofikia miaka kama 18 hivi. Jadilini Jinsi ya kutokuwa mtu wa 'sheria' (legalistic) na uvaaji kwa adabu kikawa kimungu chetu.

Yasemekana wanaume wanajaribiwa kumtamani mwanamke na mwanamke anajaribiwa kumjaribu mwanamume amtamani. Jadilini hili. (Man is tempted to lust after a woman, and a woman lusts to be lusted after).

Je, anapenda ampendeze Mungu kwa uvaaji wake au anapenda ajiletee utukufu na watu wamwangalie? Je!, anapokea mashauri kwenye uvaaji au anajivalia chochote kinachomfurahisha? Je, anajua jinsi macho ya wanaume yanavyotazama mavazi na wanavyofikiri wanapoona mwanamke amevaa kwa namna fulani? Je, anawalinda wanaume wasiwe na mawazo ya dhambi kwa uvaaji wake? Je, anavaa nguo zinazomfunika au anapenda kujionyesha mwili wake? (expose body).

Je, anavaa kama msichana au anapenda avae kama mvulana? Je, anapenda kutongoza wanaume kwa uvaaji wake, tabia na maneno? Je, anazidisha kuvaa kwa adabu mpaka anaonekana vibaya na kama si msichana? (overdo modesty). Je, ana kiburi kwamba anavaa kwa adabu na anamjaji kila mtu anayevaa vibaya? Je, anakuwa mtu wa sheria 'legalistic' kwenye uvaaji wake, akishikilia mambo ya nje, bali ndani ya moyo wake kuna roho ya uasi? Je anaweka sheria zake za uvaaji mzuri kwa wengine? (impose legalistic starndards of dress o f others).

"Mume wake hujulikana malangoni, aketipo pamoja na wazee wa nchi;" fungu la 23. Huyu mwanamume anayeheshimiwa malangoni, lazima awe anaheshimiwa nyumbani pia. Mithali 12:4. Mwanamke mwenye hekima anayemheshimu, anamsaidia mume kukomaa na kukua katika uongozi na kuchukua majukumu.

Kumheshimu mume, kunaanza msichana akiwa mdogo, kwa kumheshimu baba yake. Kutona tona (nagging) ni tabia ya kuepuka. Lazima ajifunze kuheshimu, na kuona baba na mama yake ni mamlaka yaliyowekwa na

Mungu katika maisha yake. Ajifunze kuitika kwa adabu anapoitwa na baba yake, amsaidie baba yake kumpokea mlangoni, kuchukua koti lake, kumpikia chakula chake na kumtengea. Ajifunze kumshukuru baba yake, na kujua vile vitu vinavyomfurahisha, kama vile gazeti, muziki, au vitabu. Andika orodha ya vile vinavyomchukiza na kumpendeza baba yako.

Someni kitabu cha Mithali na kuona uhusiano katika ya mzazi na mtoto. Pia someni Efeso 5:33.

Je, ni kitu gani kinaonyesha heshima kwa baba yako? Je, mama anamheshimuje baba? Hapa sisi wanawake lazima tujitahidi ili watoto wetu waone. Je, tunawasaidiaje waume zetu kama wasaidizi? Je, anawezaje kuonyesha heshima kwa babu yake au kaka zake? Je, mwaweza kuandika orodha ya vitu vinavyoonyesha kukosa adabu? Kama binti ana shida ya kuheshimu wazazi aandike sababu za kutowaheshimu, na kuona Biblia inasemaje kuhusu hizi sababu.

Soma yahusuyo mke wa Ayubu, Mikali, na Vashti, walikosaje heshima kwa waume zao? Soma Sara, na Esta waliheshimuje waume zao? Chunguza watoto au wanawake wanaokosa heshima kwa waume au wazazi wao. Je, watoto wanapata mfano gani kutoka kwa wanawake wanaokosa adabu kwa waume zao? Je, mamlaka ya mwanamume yanakuaje katika nyumba hii? Je, mamlaka ya Mungu yanakuwaje katika nyumba hii?

Binti ajadili na baba yake umuhimu wa kumheshimu mume. Je, mfanyakazi, raia, mtoto au mke afanyeje endapo mamlaka haijiheshimu? Yaani haisitahili heshima yake (unworthy of respect). Je, yuko huru kutiii mamlaka, hata inapofanya dhambi?

Je, anazungumza kwako na kwa baba yake kwa adabu? Je, anazungumza kwa maneno ya adabu kwa wazazi na kwa mamlaka? Je, unapozungumza naye au kumwita anaitikia na kugeuza uso wake akusikilize? Je, uso wake na mwonekano anaonyesha anatii? (expressions, gestures, and posture). Je, anakuheshimu mbele ya watu na hata mkiwa peke yenu? Je, anasema madhaifu yako mbele ya watu wengine? Je, anakukosoa mbele ya watu? Je, anaheshimu watu wazima polisi na viongozi wa serikali? Je, anajitahidi akupendeze? Je, anakuona wewe kama mamlaka ambayo Mungu amemwekea katika maisha yake? Je, anaheshimu maoni yako? Je, anajua jinsi ya kukueleza pale anapotofautiana nawe? Je, anakukosea adabu  na kuonyesha kwamba anaona aibu wewe kuwa mzazi wake? Je, anapenda kukukebehi au kukucheka mbele ya watu?

Kumsapoti mume ni muhimu sana, hebu wasichana wafundishwe.  Hii inafanya waume zetu kufanya shughuli yao ya uongozi waliyopewa na Mungu kwa ubora zaidi. Mwanamke ni msaidizi, wa mume wake, anapaswa kumtii na kutumia  muda na uwezo wake kumheshimu mume wake. Akifanya hivi vyema aweza kuwa taji kwa mume wake. Pengine inabidi aweke kando matakwa yao ili kuwahudumia waume zao, na hili wajifunza wakiwa wadogo.

Pengine wanawake wengine hawafikiri hili, kwa vile wameolewa na wanaume wasiomcha Mungu, ila hata hao wanahitaji kuheshimiwa; Math 20:28. Hata mwana wa Adamu alikuja kutumikia watu. Hebu ajue jinsi ya kutumikia wadogo zake, dada au kaka zake. Amuulize mama yake au mama wengine kwamba “Magoli yako leo ni nini?” Ataona magoli ya mama wengi ni ya kuhudumu, na kutumikia nyumba zao.

Ajifunze jinsi ya kupendeza kaka zake, au dada zake kwa siku moja.

Awaombee wazazi wake. Jadilini njia za kumsupoti baba kwenye shughuli zake. Je, anajua kuacha anayopenda (interest) ili kusaidia wengine? Amwangalie mama yake aone anayofanya kumsupport baba yake. Msichana amhoji baba yake ni kwa njia ipi mama alimtia moyo katika mwito wake aliopewa na Mungu. Je, amemsaidiaje katika maisha yake? Angalia jinsi mabinti wanaowasaidia baba zao. Wahoji wanaume wawili jinsi wake zao walivyowasaidia kufanikiwa kimaisha? Ni jinsi gani wamewatia moyo kukomaa katika shughuli zao za uongozi?

Soma maisha ya watu mashuhuri na viongozi wa historia na nafasi ambayo wake, au mama zao walichukua kusaidia haya? 1Tim 3:1-13.

Je, mwanamke ana jukumu kumsaidia mume wake kwa namna gani? 1Tim3 na

Tito 1 zinaonyesha kwamba mwanamume anahitaji mke kumsupport kwa mambo mengi. Angalia mfano wa Yesu kama mtumishi, alitumikiaje watu?

Angalia wanawake kwenye Biblia kama Sarah na Prisila walivyosaidia waume zao? Soma maisha ya wake kama wa Lutu, Haman, Yezebeli au Herodias; Je, walisaidiaje waume zao? Angalia familia ambayo mke hataki kumsupport mume wake, je, matokeo ni nini? Je, kwa wale wake wanaotaka kuwa na taaluma na kuiendeleza badala ya kusupoti waume wao, jiulize jinsi itakavyowasaidia watoto au waume zao.

Je, familia yawezaje kufanya dhambi kama timu? Je, mke anawezaje kuwa msaada kwa mume wake kwa maneno yake, kwa kumsifia yale mema yake, kwa kuwa mnyenyekevu na kuwa mwenye heshima, au kuwa maombi? Andikeni njia 15 za kumheshimu mume. Je, Jukumu lako kama mke lawezaje kuwa kama kanisa, msaidizi wa Kristo kwa mume wako?

Fungu la 24 latuonyesha ujasiliamali ambao mabinti zetu wanatakiwa wajifunze. Tufundishe mabinti zetu jinsi wanavyoweza kujiajiri wenyewe majumbani ili kuwa na kipato na ustadi. Baba au mama waweza kubuni mradi wa kusaidia, pengine kuuza vitu vidogo vidogo kama maji, vitu vya kushona au vya kupika. Kama kuna kazi anazoweza kuzifanya na kulipwa afanye vile.

Wanawake kama wale wa Matendo 16-15 wanatuonyesha kwamba wanaweza kuuza vitu vya nakshi. Jadilini faida za mwanamke kuwa na kazi za kumletea kipato nyumbani badala ya kufanya kazi nje ya nyumba. Jifunzeni yahusuyo leseni ya biashara na kodi ya serikali. Hoji wanawake wenye biashara zao, Je, wanafanya nini? Fikiria biashara inayohitaji mtaji mdogo na muanze. Je, mwanamke atumiaje mapato yake anayopata kwenye kazi zake?

Je akifanya kazi ina ubora? Je, anapenda Mungu afurahi na kazi yake? Je, anaongeza ustadi wa ufundi alio nao? Je, ana ustadi wa kumwezesha kupata kipato? Je, wengine wanajua ni mfanyakazi bora? Je, watu wanapenda bidhaa zake au ustadi wake? Je, ana mbinu za ujasiliamali? Je, anapenda kufanya kazi nje na nyumbani? Je, akiona hitaji anajaribu kulitatua? Je, anapenda apate pesa kwa mahitaji yake binafsi tu au kusaidia familia na wengine pia?

"Nguvu na hadhi ndiyo mavazi yake, anaucheka wakati ujao;" fungu la 25. Mwanamke huyu anajua maisha ya imani, kuridhika na kumshukuru Mungu. Anajua Mungu ameshika hatamu ya wakati ujao. Twahitaji kuwasaidia mabinti kuridhika na yale ambayo Mungu, na sisi wazazi tumewapa. Twaweza kujadili na kuandika pamoja yale ambayo tunashukuru kwayo. Je, anawashukuru wazazi wake kwa yapi? Kuna tofauti gani kati ya kuomba na kushukuru? Filipi 4:6-7 na 1

Thes 5:16-18. Je, ana wivu, au chuki?

Soma watu ambao hawakuridhika kwenye Biblia. Kila mara unapojaribiwa kulalamika, soma Wafilipi 2 na Isaya 53. Je, binti ya Mfalme anapaswa kuishi maisha ya kutoridhika? Zungumza na mwanamke mtu mzima kuhusu kuridhika. Jadili neno kutamani (covet) lina maana gani? Andikeni orodha ya vitu ambayo hamridhiki navyo (discontent); kwa mwonekano wako, unapoishi, familia yako, kisha andika shina la kutoridhika na hivi vitu kwenye moyo wako. Kisha ungama kwa Mungu. Angalia Waebrania 11, na jinsi kila mtu aliyeandikwa alivyoridhika.

Je, anamshukuru Mungu kwa anayompa? Je anadai kununuliwa vitu mkiwa dukani? Je, anajali kama mwingine atapata sehemu kubwa kuliko yeye? Je, anataka kuwa na vitu vile anaona wengine wanavyo? Je, anaweza aishi maisha magumu na kuona mafundisho Mungu anampa?

Je, anamtegemea Mungu kama mtoaji? Je, anakazania mambo ya kupita au ya milele? Je, anaridhika na alivyonavyo au anataka zaidi? Je, ana roho ya shukurani kwa wazazi na upendo wenu? Je, anatoa shukurani kwa huduma au anavyofanyiwa? Je, anapenda kulalamika na kulialia? Je, anajitahidi na wengine kupata anachotaka? Je, anapenda kutetea haki zake mara zote? Je, anajihurumia kupita kiasi; (self pity)? Je, anatamani vitu vya wengine na kupata wivu? Je, anatamani talanta au kufanikiwa kwa wengine? Je, anatamani baraka za wengine na zinamtia uchungu?

Mungu hutoa mahitaji yetu sasa na ya wakati ujao. Ni nani alimpa Adamu mke wake? Je, Mungu ataka tuwe watu wa namna gani? Mika 6:6-8. Angalia wanawake wote waliosaidia kazi Yesu au mahitaji yake, wangapi walikuwa hawajaolewa? Wajue wanawake ambao hawajaolewa kwenye ushirika wao na kuwatembelea. Je, binti anaweza kuifanya miaka ya kutoolewa iwe bora (shule, kusoma Bibia, huduma, kukariri mafungu, ustadi). Je! Anajua dhambi iliyoingia ya wanawake kuolewa na wanawake na wanaume kuolewa na wanaume? Jadili naye.

Biblia yataja watu kama vile Miriamu, Rahabu, Delila, Mariamu, Martha, Esta, Ana, mjane wa Serepta, binti za Zelofehadi. Je, kutoolewa kwao kuliwasaidiaje kutumika walivyotumika? Je, Mungu aliwasaidiaje kupata riziki? Makosa gani walifanya? Na adhabu gani waliyoipata? 1 Kor 7:34-35.

Andika jinsi ambavyo mwanamke asiyeolewa na asiyekuwa na jukumu la kumpendeza mume anaweza kuhudumu kwa ufanisi mkubwa. Angalia jinsi uhuru wake unavyoweza kumsaidia kuwa wa huduma kwa kazi ya Mungu. Ni mambo gani ambayo waweza kusaidia kanisa sasa ikiwa haujaolewa? Je, ukiitwa na Mungu kutoolewa (single) waweza kumtumaini Yeye?

Zungumza na wazazi kuhusu kuitwa kumtumikia Mungu pasipo kuolewa. Kwa nini Mungu, wakati mwingine huita watu ambao hawajaolewa? Je, watu hawa wanajisaidiaje kupata riziki? Je, usipoolewa utaishi kwenye mji wako mwenyewe? Je, ni wapi utaomba ushauri ukiwa mwenyewe (single)? Soma Biblia inapozungumzia: “Mwito wa kuishi maisha ya usela/solemba; (single). Soma kitabu; ‘Did I Kiss Marriage Goodbye;’ cha Caroly MCCulley. Je, maisha ya kuishi mwenyewe yanaweza kuwa bora na kamili? Jadilini kuhusu upweke.

Je, anamtumaini Mungu kwa kila jambo na anaridhika (fulfillment) na uhusiano wake na Mungu? Je, anajua adui anakuja kwa njia nyingi zaidi ya ile ya kutenda dhambi? Kukata tamaa, unafiki, marafiki wabaya, kuchoka; n.k. Je, amejitoa kwa Mungu kutumikia wengine, na anatumia nafasi hiyo

kuanzia nyumbani? Je, ana nafasi nyumbani kujifunza kuwa mke na mama? Je, anamtumaini Mungu kumchagulia mume na anayefaa kwa wakati unaofaa, kama ndio mpango wake? Je, anajali mawazo yako kuhusu wavulana wanaokuja kwake? Je, anajali mambo ya kuolewa kuliko utii kwa Mungu? Je, ana ndoto za mchana kuhusu ndoa? Je, ana mawazo ya mahaba yasiyofaa?

Je, kipi ni muhimu kwake, kuwa mcha Mungu aliyekomaa au kuolewa na mtu yoyote? Je, anaona wivu rika zake wakiolewa? Je, anapata hofu akijua hataolewa? Je, anajua kwamba Mungu anaweza kuwa amempa wito wa useja na kumtumikia badala ya kuolewa? Je, anajua kwamba Mungu ana mipango maalumu naye, endapo akiolewa au asipoolewa? Je, anatumia miaka ya kutoolewa ni ya kujitayarisha kwa wito mkuu wa Mungu? Je, anazungumza na wanawake wasioolewa kanisani kwa njia nzuri na upendo? Je, ana upendo wa kutaka kushugulikia mahitaji ya wale wapweke?

Tufundishe mabinti zetu kutoishi maisha ya hofu, bali nguvu na ujasiri. Watambue kuomba ni muhimu. Wanapopata hofu wamtegemee Yeye. Someni kuhusu ahadi za Mungu na ulinzi wake. Angalia wanawake hawa walimtumainije Mungu, mke wa Nuhu, mke wa Lutu, Sara, Esta, Yokebedi, Debora au za Ruth. Chagua Zaburi za kusoma pale unapokuwa na woga. Angalia pale wana wa Israeli walipopata hofu kwenye kitabu cha Kutoka. Je, wale wa Waebrania 11 walionyeshaje ujasiri?

Wahoji wanawake kadhaa pale walipojaribiwa kuwa na hofu na ilikuwaje walipoogopa na ilikuwaje walipomtegemea Mungu? Soma maisha ya Sara, mazuri na madhaifu yake yalikuwa yapi? Je, alifanyaje alipojaribiwa? Je, kwa nini ametolewa mfano kwa wale wenye imani?

Je, ana hofu ya kumtumaini Mungu kumtunza? Je, ana imani ya Warumi 8:28? Je, anajua mafungu ya kusoma akiwa na woga? Je, akiwa na woga anaomba? Je, anaogopa kujaribu chochote kipya? Je, anaogopa watu wanavyomfikiria? Je, anaogopa kufanya makosa? Je, anaogopa wakati ujao (future) Je, anaweza kusema 'hapana' watu wakimwambia atende uovu? Je, anaogopa kujeruhiwa? Je, anaogopa kuzungumza na watu? Je, ana wasiwasi, na kuona kwamba atashindwa, na kuona matatizo tu?

Je, ana ujasiri wa kutatua magomvi au kutoelewana na marafiki, ndugu, walimu au wazazi? Je, ana ujasiri kusema alikosea? Je, yupo tayari kuomba msamaha akimkosea mtu? Je, anamwogopa Mungu zaidi ya binadamu? Je, anaweza kumwambia rafiki akifanya dhambi? Je, anakata tamaa afanyapo dhambi? Je, anapokea maonyo na kukosolewa kwa hali chanya? Je, anaogopa kutoa mawazo yake? Je, anaogopa kumshuhudia Kristo mbele ya watu? Je, ana hofu kuelezea hisia zake?

"Hufumbua kinywa chake kwa hekima; na sheria ya wema i katika ulimi wake." Ulimi hauwezi ukafungwa, una uovu usiotulia. Umejaa sumu iletayo mauti. Kama wazazi twapaswa tuwasaidie watoto 'kufuga' ulimi mapema ili wawe mibaraka kwa waume zao, watoto, kanisa na jumuiya. Daudi anamwomba Mungu atie kufuli ulimi wake. Ni vizuri tuwaambie mabinti zetu pale wanapozungumza isivyo, na marafiki zao waweza kuwa walinzi wao pia. Twapasa tusirudishe ubaya kwa ubaya. Twawezaje kufanya hivi? Mwambie binti amuulize mtu amwangalilie yale maneno yote yasiyo na sababu (idle words ya Mathayo 12:36-37).

Someni Yakobo 3 pamoja na kujadili. Soma watu ambao wamewasaidiwa

kwa maneno mazuri, na wale ambao maneno mabaya yamewaharibia. Angalia maneno kama magomvi, malamiko, umbeya, uongo, kutia chumvi, kushuhudia uongo, na kukufuru. Je, mwanamke anawezaje akajitawala kwa maneno yake? Soma kisa cha Abigaili au mke wa Pilato. Je, mwanamke awezaje kuwa na maneno ya kutia moyo au ushauri mwema? Twawezaje kutawala nafsi tunapozungumza? Twawezaje kufanya mazungumzo yetu yakawa mbaraka (improving speech)?

Je, anapenda kuwabandika watu majina? Je, anazungumza kwa ujinga, kwa sauti inayokera? Je, anakebehi wengine(mock)? Je, anapenda kulialia na kulalamika? Je anapenda kusengenya wengine? Je, sauti yake inakuwa kali wakati wote? Je, anapiga mayowe akigombana na nduguze? Je, anapenda kuripoti makosa ya wengine? Je, anatumia maneno yasiyo na upendo (unkind) kwa nduguze? Je, anapenda kusema maneno ya kuchokoza wenzake? Je, anapenda kukosoa watu na kuwakejeli au kuwashushua (sarcastic)?

Je, anapenda kulitaja Jina la Mungu bure? Je, anaonyesha heshima kwako na baba yake kwa maneno yake? Je, maneno yake yanajenga wengine au yanawararua? Je, anasema lolote limjialo kichwani au anachuja maneno? Je, anamsahihisha aliyekosea kwa unyenyekevu? Je, anatoa ushauri mwema kwa wengine? kufungua kinywa kwa hekima kwa mama au mke ni muhimu. Watoto wanabidi wafundishwe (training) kutii. Hapaswi kuwa mvivu kwa kazi . Twapaswa kufundisha binti zetu jinsi ya kuwa na urembo wa ndani zaidi ya wa nje.

Masakamomadi-Jersey 2012.

Biblia inataja maagano saba makuu ambayo Mungu amefanya na watu:
Agano la Kwanza—Adamu (Mwanzo 1–3)
Agano la Pili—Nuhu (Mwanzo 6–9)
Agano la Tatu—Abrahamu (Mwanzo 12:1–3)
Agano la Nne—Musa na taifa la Israeli (linalojulikana kama Agano la Sinai au Agano la Musa; Kutoka 19-24)
Agano la Tano—Finehasi ( Hes. 25:10–13 )
Agano la Sita—Daudi ( 2 Sam. 7:5–16 )
Agano la Saba—Agano Jipya ( Yer. 31:31–34 )
Soma maandiko yafuatayo. Wanamaanisha nini wanaposema “Agano la milele”? Mwa. 9:16, 17:7, Isa. 55:3, Ebr. 13:20.
Tunaungana pamoja kwamba Yerusalemu mpya haiko katika mahame au magofu kama wakati wa Nehemia, Ezra, Esta na Zerubabeli, yaani tunatazamia mbingu na nchi mpya.

# MASOMO
# ya BIBLIA
# NA HABARI
# ZA KUSHANGAZA

## MAMBO YA AJABU MAFUNZO YA BIBLIA KWA KILA MWANADAMU, na HASA VIJANA

## MAFUNZO YA BIBLIA
### Katika Nyakati Hizi Zenye Changamoto za Kimaadili

### Somo la 1

Katika nyakati hizi zenye changamoto za kimaadili - ambapo mabilioni ya watu huibiwa kwa njia ya ulaghai na mashirika yanayoaminiwa, viongozi wa kiroho huthibitisha uongo wanaposema uwongo katika siasa na hili linaonekana kuwa jambo la kawaida wakati wale unaowategemea mara nyingi wanakuumiza zaidi - je, kuna chochote kilichosalia ambacho wewe unaweza kukiamini? Ndiyo! Unaweza kuitumaini Biblia kabisa! Kwa nini? Angalia tu ushahidi...
Biblia si mkusanyo wa mawazo ya wanadamu. Waandishi wake waliongozwa na Roho Mtakatifu.

**1. Biblia inadai nini kujihusu?**
Biblia inasema, “Kila andiko lenye pumzi ya Mungu.” 2 Timotheo 3:16 . “Unabii haukuletwa kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu. 2 Petro 1:21 . “Maandiko hayawezi kuvunjwa.” Yohana 10:35 .

**Jibu:** Inadai kuwa imevuviwa. Iliandikwa na watu ambao waliongozwa na Roho Mtakatifu. Haiwezi kubatilishwa, kuvunjwa au kuthibitishwa kuwa si Kweli.
Yesu alinukuu Biblia na kusema kwamba ilikuwa Kweli.

**2. Je, Yesu alionyeshaje ujasiri na imani Yake katika Maandiko?**
Yesu alisema, “Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu.” “Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana, Mungu wako.” “Imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye peke yake.” Mathayo 4:4 , 7 , 10 . “Neno Lako ni Kweli.” Yohana 17:17 .

**Jibu:** Yesu alinukuu Maandiko alipokutana na majaribu ya Shetani. Pia alisema kwamba Biblia ni Kweli Yohana 17:17. Yesu mara nyingi alinukuu Maandiko kama mamlaka ya Ukweli aliokuwa akifundisha.
Kabla ya Koreshi kuzaliwa, nabii wa Mungu wa Biblia alimtaja kuwa jenerali ambaye angepindua Babeli/Babiloni takribani miaka 150 kabla.

**3. Je, unabii wa Biblia unathibitisha kwamba ulivuviwa na Roho Mtakatifu?**
Biblia inasema, “Mimi ni Bwana ... nayahubiri mambo mapya; kabla hayajatokea nawaambia ninyi habari zake.” Isaya 42:8 , 9 . “Mimi ni Mungu ... nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo ambayo hayajafanyika bado.” Isaya 46:9 , 10 .

**Jibu:** Utabiri wa Biblia wa mambo yatakayotokea wakati ujao unathibitisha uvuvio wa Maandiko jinsi yanavyotimia. Angalia mifano ifuatayo ya unabii wa Biblia

uliotimizwa:
Milki nne za ulimwengu zitatokea: Babeli, Umedi-Uajemi, Ugiriki, na Roma Danieli sura ya 2, 7, 8 .
Koreshi kuwa shujaa wa kuiteka Babeli Isaya 45:1-3 .
Baada ya Babiloni kuharibiwa, haingekaliwa tena Isaya 13:19 , 20. Yeremia 51:37.
Misri haingekuwa tena na cheo cha kuamuru kati ya mataifa Ezekieli 29:14 , 15 30:12 , 13 .
Misiba yenye kutikisa dunia na hofu kuelekea mwisho wa wakati Luka 21:25 , 26 .
Kushuka kwa maadili na kuzorota kwa hali ya kiroho katika siku za mwisho 2 Timotheo 3:1-5 .

**4. Je, tunaweza kutazamia kwamba taarifa za kisayansi zinazotolewa katika Biblia ziwe sahihi?**
Biblia inasema, “Neno Lako ni Kweli tangu mwanzo.” Zaburi 119:160 . “Roho ... atawaongoza awatie kwenye Kweli yote.” Yohana 16:13 .

**Jibu:** Ndiyo, Biblia ni Kweli. Roho Mtakatifu, ambaye aliwaongoza waandishi wa Biblia, husema Ukweli sikuzote. Hapa kuna maelezo machache ya Biblia ambayo yamethibitishwa na sayansi:
“Yeye ... aitundika dunia juu ya utupu (pasipo kitu).” Ayubu 26:7 . Jambo hilo la kisayansi limetoka kwa Ayubu, kitabu cha kale zaidi cha Biblia.
“Yeye ... ameketi juu ya duara ya dunia.” Isaya 40:22 . Biblia ilisema dunia ni duara karne nyingi kabla ya mwanadamu kujua.
“Kufanya uzito kwa upepo.” Ayubu 28:25 . Muda mrefu kabla ya wanasayansi kujua, Mungu alisema hewa ina uzito.
“Kwa Yeye [Yesu] vitu vyote hushikana.” Wakolosai 1:17 . Neno hili “jumuisha” hapa kihalisi linamaanisha “kushikilia pamoja” au “kushikamana.” Tafsiri nyingi za Biblia zinaiweka “shikamana pamoja.” Hili ndilo jibu la swali la kutisha la wanafizikia wa nyuklia kuhusu atomu. Siri ya kweli ya atomi haihusishi nguvu yake kuu (mega), lakini badala yake, “Kwa nini atomi haijitenganishi au haisambaratiki?” Maarifa ya kisayansi yanasema vipande havipaswi kushikana pamoja, lakini sivyo ilivyo hali halisi. Wanasayansi wengine wanashangaa ni nguvu gani ya kushangaza, ambayo haijulikani kwao kabisa, inashikilia hizi atomi pamoja. Biblia inasema kwamba nguvu za ajabu ni Muumba, Mungu Mwenyewe.

Magonjwa mengi yasingekuwapo ikiwa sheria za kale za Mungu kuhusu maadili zingefuatwa.

**5. Je, kanuni za afya za kibiblia zimeelekezwa kwa akili ya karne ya ishirini na moja? Ndiyo!**

**Jibu: Kufu**unika uchafu wa kinyesi- Kumbukumbu la Torati 23:12 , 13 .
Utoaji wa Biblia wa siku za Musa kwamba uchafu wa mwili uzikwe ulikuwa miaka 3,500 kabla ya wakati wake na uliokoa maelfu ya maisha yasiyohesabika ya Wayahudi. Matatizo makubwa bado hutokea wakati usafi wa mazingira haujashughulikiwa ipasavyo.
“Wala tusifanye uasherati.” 1 Wakorintho 10:8 .

Neno "uasherati" lamaanisha kila aina ya mwenendo mpotovu wa kingono. Hakungekuwa na mlipuko wa UKIMWI ikiwa shauri hilo la kisasa la Biblia lingetiiwa, wala utoaji-mimba haungekuwa kashfa ya kimataifa kama ilivyo sasa.
Acha kunywa vinywaji vyenye kileo Mithali 23:29-32 .
Ikiwa suluhu hii yenye ufanisi mkubwa ya Biblia ingetekelezwa, hebu fikiria matokeo yake yangemaanisha nini:
Mamilioni ya waraibu wa ulevi wangekuwa raia wenye kiasi, na wenye kuheshimika.
Mamilioni ya familia yangeungana pamoja tena.
Mamilioni ya nyumba zilizovunjika zingelirekebishwa.
Maelfu ya maisha yangeokolewa kwani watu wangeendesha magari kwa kiasi au wakiwa na akili timamu.
Maelfu ya viongozi wa serikali, wafanyabiashara na wataalamu wangefanya maamuzi yaliyo na busara kwasababu ya utimamu wa akili.
Mabilioni ya dola yangepatikana kwa matumizi ya wanadamu.

Utumiaji wa pombe umeleta ole isioelezeka kwa watu wengi.

**Kumbuka:** Mungu sio tu anatuambia jinsi ya kufanikiwa kwa furaha katikati ya matatizo ya leo ya kutisha, lakini pia anatupa nguvu za ajabu ili kutuwezesha kufanya hivyo ( 1 Wakorintho 15:57 , Wafilipi 4:13 , Warumi 1:16 ). Kanuni za afya za Biblia zinafaa na zinahitajika sana, lakini ni wachache wanaozisikiliza. Kwa habari zaidi kuhusu afya, angalia Mwongozo wa 13 wa Utafiti.

Vitu vya kale vilivyochimbuliwa na wanaakeolojia huthibitisha tena na tena usahihi na Ukweli wa Biblia.

**6. Je, maelezo ya kihistoria ya Biblia ni sahihi?**
Biblia inasema, "Mimi, Bwana, nasema Kweli, natangaza yaliyo haki." Isaya 45:19, UV.

**Jibu:** Ndiyo, taarifa za kihistoria za Biblia ni sahihi. Anachosema Mungu katika kitabu Chake ni Kweli. Nyakati nyingine, kwa muda, huenda usipatikane ushahidi wa kuthibitisha mambo fulani ya kihistoria kutoka katika Biblia, lakini baada ya muda uthibitisho huo huonekana. Zingatia yafuatayo:
Kwa miaka mingi watu walio na shaka walisema kwamba Biblia haiwezi kutegemewa kwa sababu inataja taifa la Wahiti Kumbukumbu la Torati 7:1 na majiji kama Ninawi Yona 1:1 , 2 na Sodoma Mwanzo 19:1 , ambayo walikana kuwa hayajawahi kuwepo. Lakini sasa akeolojia ya kisasa imethibitisha kwamba zote tatu zilikuwepo (akeolojia ni machimbo ya mambo ya kale ili kupata vitu vinavyothibithisha historia ya mambo yaliyopita).
Wachambuzi pia walisema kwamba wafalme Belshaza katika Biblia Danieli 5:1 na Sargoni Isaya 20:1 hawakuwapo kamwe. Kwa mara nyingine tena, sasa imethibitishwa walikuwepo.
Watu wenye kutilia shaka pia walisema rekodi ya Biblia ya Musa haikuwa yenye kutegemeka kwa sababu wazungumzia na kuandika katika Kutoka 24:4 juu ya magari ya magurudumu Kutoka 14:25 , nao wanasema kwamba hayakuwako

wakati huo. Wao, bila shaka, wanajua vizuri zaidi leo.
Wakati fulani wafalme 39 wa Israeli na Yuda ya kale waliotawala wakati wa ufalme uliogawanyika walithibitishwa tu na rekodi ya Biblia, kwa hiyo wachambuzi walidai hizi ni habari za uongo. Lakini wanaakiolojia walipata maandishi ya kikabari/ cuneiform yaliyotaja wengi wa wafalme hao na, kwa mara nyingine tena, rekodi ya Biblia ilithibitishwa kuwa sahihi. Wakosoaji wamethibitishwa mara kwa mara kuwa kile Biblia ilikisema ni sahihi kwani uvumbuzi mpya unathibitisha haswa watu wa Biblia, mahali, na matukio. Jambo hilo litakuwa hivyo daima.

*The Revised Standard Version of the Bible C 1946, 1952, 1971 na Idara ya Elimu ya Kikristo ya Baraza la Kitaifa la Makanisa ya Kristo nchini Marekani. Imetumika kwa ruhusa.

**7. Mojawapo ya miujiza mikuu ya Biblia ni umoja wake. Tafadhali tafakari mambo ya ajabu yafuatayo:**

**Jibu:**

A. Vitabu 66 vya Biblia viliandikwa:
Katika mabara matatu.
Katika lugha tatu.
Na takriban watu 40 tofauti wafalme, wachungaji, wakulima, wanasayansi, mawakili, jemadari wa jeshi, wavuvi, makuhani, na tabibu.
Kwa kipindi cha takriban miaka 1,500.
Juu ya mada zenye utata zaidi.
Na watu ambao, katika hali nyingi, hawajawahi kukutana.
Na waandishi ambao elimu na asili yao ilitofautiana sana.

B. Walakini, ingawa inaonekana kuwa haiwezekani kabisa,
Vitabu 66 vinadumisha upatanifu kati yao.
Mara nyingi dhana mpya kuhusu jambo fulani huonyeshwa, lakini dhana hizo hazipunguzi yale ambayo waandishi wengine wa Biblia husema kuhusu jambo hilohilo.

C. Yaani ukizungumzia kuhusu mambo ya kushangaza, hapa ndiyo umefika kwenyewe!

Waulize watu ambao wameona tukio linalofanana na kisha kila mmoja atoe ripoti ya kile kilichotokea. Utaona kwa jinsi ambayo wanatatofautiana sana na kwa hakika daima watapingana kwa namna fulani. Lakini Biblia, iliyoandikwa na waandishi 40 katika kipindi cha miaka 1,500, nayo inasomwa kana kwamba imeandikwa na akili moja kuu. Na, kwa hakika, ilikuwa hivyo: "Watu watakatifu wa Mungu walinena wakiongozwa na Roho Mtakatifu." 2 Petro 1:21 . Roho Mtakatifu "aliwaongoza" wote. Yeye Ndiye Mwandishi na Mbunifu halisi wa Biblia. Nyakati nyingine zile Injili nne hutofautiana katika jinsi zinavyoripoti tukio moja, lakini zinakamilishana kabisa.

Kumkubali Kristo na kutii Maandiko humbadilisha mlevi, mchafu, mwovu, mwenye dhambi kuwa Mkristo mwenye upendo, kiasi, na safi. Wanaoshuku hawawezi kueleza Ukweli huu.

**8. Ni uthibitisho gani wa uvuvio wa Biblia unaopatikana katika maisha ya watu?**
Biblia inasema, “Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama, yamekuwa mapya.” 2 Wakorintho 5:17 .
Wakristo wana furaha ya ndani na amani ambayo wengine hawana.

**Jibu:** Maisha yaliyobadilika ya wale wanaomfuata Yesu na kutii Maandiko ni uthibitisho wenye kuchangamsha moyo Zaidi, wa uvuvio wa Biblia. Mlevi anakuwa na kiasi; wasio na maadili, safi; waraibu, huru; wasio wa dini, wacha Mungu; waoga, jasiri; na wasio na adabu, wa fadhili.

Mkosoaji wa Marekani alikuwa akitembelea kisiwa ambacho wenyeji wake walikuwa wanakula nyama  za watu. Alipomwona mzee akisoma Biblia, alimdhihaki kwa kusoma kitabu “kilichojaa hekaya ambazo tayari zilikuwa zimefichuliwa kwamba si sahihi.” Mzaliwa huyo alitabasamu na kusema, “Rafiki yangu, shukuru kwamba tunaamini kitabu hiki. La sivyo, tungekuwa tunakuhudumia kwa chakula cha jioni leo.” Biblia hubadili watu kwelikweli, na jambo hilo la kustaajabisha linathibitisha kwamba ilivuviwa na Mwenyezi Mungu.

**9. Ni ushahidi gani wa uvuvio wa Biblia ambao unaojitokeza tunapolinganisha unabii wa Agano la Kale wa kuja kwa Masihi na matukio ya Agano Jipya katika maisha ya Yesu?**
Biblia inasema, “Akianzia Musa na manabii wote, [Yesu] akawaeleza katika Maandiko yote mambo yaliyomhusu Yeye Mwenyewe. Luka 24:27 . “Kwa maana [Apolo] kwa nguvu aliwakanusha Wayahudi hadharani, akionyesha kutoka katika Maandiko kwamba Yesu Ndiye Kristo.” Matendo 18:28 , NKJV .*
Yesu alitimiza zaidi ya unabii 125 wa Agano la Kale kuhusu Masihi.

**Jibu:** Utabiri wa Agano la Kale wa kuja kwa Masihi ulikuwa mahususi na ulitimizwa kwa uwazi sana na Yesu wa Nazareti hivi kwamba Yesu na Apolo walitumia unabii huu ili kuwathibitishia Wayahudi kwamba Yesu alikuwa Kweli Masihi. Kuna zaidi ya 125 ya unabii huu. Wacha tupitie 12 tu kati yao:

| Unabii | | Maandiko ya Agano la Kale | Utimilifu wa Agano Jipya |
|---|---|---|---|
| 1. | Kuzaliwa wa Bethlehemu | Mika 5:2 | Mathayo 2:1 |
| 2. | Kuzaliwa na bikira | Isaya 7:14 | Mathayo 1:18-23 |
| 3. | Atakuwa wa ukoo wa Daudi | Yeremia 23:5 | Ufunuo 22:16 |
| 4. | Jaribio la Yeye kuuawa na Herode | Yeremia 31:15 | Mathayo 2:16-18 |
| 5. | Kusalitiwa na rafiki | Zaburi 41:9 | Yohana 13:18 , 19 , 26 |
| 6. | Anauzwa kwa sarafu 30 za fedha | Zekaria 11:12 | Mathayo 26:14-16 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | Kusulubiwa Msalabani | Zekaria 12:10 | Yohana 19:16-18 , 37 |
| 8. | Kura kupigwa kwa nguo Zake | Zaburi 22:18 | Mathayo 27:35 |
| 9. | Hakuna mifupa iliyovunjika | Zaburi 34:20 Kutoka 12:46 | Yohana 19:31-36 |
| 10. | Alizikwa kwenye kaburi la tajiri | Isaya 53:9 | Mathayo 27:57-60 |
| 11. | Mwaka, siku, saa ya kufa Kwake | Danieli 9:26 , 27 Kutoka 12:6 | Mathayo 27:45-50 |
| 12. | Kufufuka siku ya tatu | Hosea 6:2 | Matendo 10:38-40 |

Dk. Peter Stoner, mwenyekiti wa zamani wa idara za hisabati, astronomia, na uhandisi katika Chuo cha Pasadena California, alifanya kazi na wanafunzi 600 kwa miaka kadhaa akitumia "kanuni ya uwezekano" yaani mahesabu ya probability kwa unabii wa kuja kwa Masihi. Walichagua nane tu kati ya nyingi zilizopo na hatimaye kuamua nafasi ya Zote nane kutimizwa kwa mtu mmoja katika maisha ni uwezekano wa moja kati ya 1,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000. Je, uwezekano wa ule unabii zaidi ya 125 wa Masihi ungekuwaje? Hilo Halingeweza kutokea tu hivyo kama bahati!

*The Holy Bible, New King James Version, C 1979, 1980, 1982 na Thomas Nelson, Inc. Imetumiwa kwa ruhusa.
Biblia inafundisha kwamba dunia iliumbwa kwa siku sita halisi.

**10. Mtu anayekubali Biblia kuwa Neno la Mungu lililoongozwa na roho anapata faida gani kubwa?**
Biblia inasema, "Nina ufahamu kuliko wazee, kwa kuwa ninayashika mausia Yako." Zaburi 119:100 . "Wewe ... umenifanya kuwa na hekima kuliko adui zangu." Zaburi 119:98 . "Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, ndivyo ... mawazo Yangu [ya juu] kuliko mawazo yenu." Isaya 55:9 .

Simulizi la Biblia kuhusu Gharika hutoa majibu ambayo wasomi wa ulimwengu wanatafuta.

**Jibu:** Mtu anayekubali Neno la Mungu hivi karibuni atajua majibu ya changamoto nyingi ngumu ambazo wasomi wa kilimwengu hawataweza kuzipata. Kwa mfano, Biblia inafundisha:
Mungu aliumba dunia na viumbe vyote vilivyo hai katika siku sita halisi za saa 24 Kutoka 20:11. Zaburi 33:6, 9 .

Gharika ya ulimwenguni pote iliharibu kila kiumbe hai isipokuwa viumbe vya baharini na vilivyokuwa ndani ya safina ya Nuhu Mwanzo sura ya 6, 7, 8.
Lugha mbalimbali za ulimwengu zilianzia kwenye Mnara wa Babeli Mwanzo 11:1-9.
Mungu, ambaye amekuwepo siku zote na anajua kila kitu, anashiriki na si kweli tatu zilizo hapo juu, akitambua kwamba hatungeweza kamwe kuzitambua sisi wenyewe. Tunajua "kwa sehemu" tu sasa 1 Wakorintho 13:9 . Na ujuzi wa Mungu "umepita ufahamu/

ujuzi." Warumi 11:33 . Wale wa uibukaji hawatawahi kujua umri wa dunia kwa sababu iliumbwa na umri unaoonekana na kujulikana, kama vile Adamu na Hawa walivyokuwa.

Wanandoa hao walikuwa na umri wa siku moja tu katika siku yao ya pili ya maisha, lakini walionekana kuwa watu wazima na wala hawakuwa na vitovu, maana hawakuzaliwa bali waliumbwa na Mungu. Vyombo vya kupimia vya mwanadamu haviwezi kuruhusu umri uonekana, kwa vile havijui, na hakuna mwenye kujua isipokuwa Mungu. Katika hali kama hizi basi, vyombo hivyo havina uaminifu. Amini Biblia, na daima utakuwa mbele ya mawazo ya wasomi wa ulimwengu na wenye hekima ya kidunia.

**11. Ni matukio gani muhimu ya ulimwengu ambayo yamekazia sana nguvu na rejelea/rufaa ya Biblia?**

**Jibu**: Kushindwa na kuporomoka kwa ukomunisti na kudhoofika na kutopatana kwa nadharia ya uibukaji kumeangazia Biblia.

Sayansi ya Kweli sikuzote inapatana na Biblia kwa sababu Mungu Ndiye mwandishi wa yote mawili. Twende kwa Mungu ili kujua sayansi ya Kweli, na kurejelea sayansi ya mwanadamu pale tu inapopatana na Biblia! Chanzo cha Sayansi ni Mungu, Wanasayansi wanaendelea kuvumbua vitu, na vingine walivyofanya makosa wanatuambia kwamba hapa ilikosewa. Mungu haendelei kuvumbua, YEYE Ndiye aliyeumba. Je, pale ulipo leo unaona sokwe wa Gombwe Tanzania au Gorila wa virunga Congo wakiendelea kubadilika kuwa watu na kuingia kwenye nyumba na kuanza familia? Sayansi inasema viumbe vidogo kama minyoo huwa sokwe na kisha watu, mbona hatuoni jambo hili likiendelea? Na historia yetu ya vitabuni tunavyofundishwa ina miaka kama 5000 hivi kutoka Mesopotamia, Je yale mamilioni ya miaka wanayosema yako wapi, na nini kilitokea siku zile? Hakuna rekodi yoyote kabisa!

**Kumbuka:** Muungano wa Jamhuri za Kisoshalisti za Kisovieti ulijaribu ukomunisti, ukafiri/atheist, na pia uibukaji, ambayo ndiyo kanuni kuu ya Ukarl Marx. Wote walishindwa. Tokeo la demokrasia mpya hutambua kwamba ni jambo moja tu litakalofanya kazi, na karibu kwa sauti moja wanalilia Jumuiya ya Wakristo: "Tuleteeni Biblia na mahubiri na mafundisho ya Kikristo. Sisi ni lazima sasa tujenge juu ya msingi usiotikisika wa sala na imani ya Kikristo. Hakuna kitu kingine kitakacholinganishwa na hichi. Wala hakuna kitu kingine chochote ambacho kitajibu maswali makuu ya maisha na kuleta amani katika mioyo ya watu wetu. Tafadhali usitufanye tungojee! Tunatamani sana na tunahitaji Biblia, Mungu, na Ukristo sasa hivi." Kwa mara nyingine tena, Neno la Mungu limeshinda.

Uibukaji, kama ulivyokuwa ukomunisti, umepoteza mshikamano wake na uaminifu. Ni lazima tukumbuke kwamba haina chochote zaidi ya kuwa nadharia isiyothibitishwa na tete. Tutataja hapa vitu vitatu pekee:
Kitabu cha Robert Gentry cha Creation's Tiny Mystery kimewavuruga wana uibukaji wengi kwa uthibitisho wake wa wazi wa uumbaji wa papo hapo. Mystery in the Rocks, kitabu ambacho ni rahisi kueleweka kulingana na utafiti wake, kinaweza

kununuliwa kutoka huduma ya Amazing Facts.

Uthibitisho wa hivi majuzi wa baiolojia wa molekuli kwamba seli moja ni ya kushangaza sana nayo hufanya asili ya kiajali na kuleta uhai katika seli moja imeonyesha upuuzi mkali wa kihisabati.

Enzi au miaka tofauti sana sasa inayowekwa kwa tabaka za shimo la Grand Canyon Marekani kwa vipimo vya sasa vya kisayansi, kinyume na vile vilivyotolewa hapo awali, huwafanya wanauibukaji na vipimo vyao vya awali kuonekana kutojali na kutowajibika. Nadharia za kumkana Mungu na kuleta uibukaji, eti kwamba wanadamu na nyani walitoka kwa mababu wamoja inadharau dhana kwamba watu waliumbwa kwa mfano wa Mungu. Inakana kuwako kwa Mungu, inamkana kabisa Yesu kama Mwokozi, inakanusha Biblia, na inadhihaki Ukweli wa makao ya milele mbinguni. Shetani anapenda nadharia ya uibukaji kwa sababu inaharibu uaminifu wa wokovu. Wakomunisti wanajifunza hiyo nadharia. Je na sisi tujihusishe na habari hizo! Hivi hatuoni kama ukomunisti ulishindwa na kupitwa na wakati, ni nani kweli anataka kuwa mkomunisti?
Biblia inavutia watu wote kwa sababu inatoa majibu yaliyo wazi kwa maswali yenye kutatanisha maishani.

**12. Kwa nini Biblia inavutia hivyo ulimwenguni pote?**
Biblia inasema, "Neno Lako ni taa na... mwanga wa njia yangu." Zaburi 119:105. "Hayo nimewaambia ... ili furaha yenu iwe kamili." Yohana 15:11 . "Kwa mfano wa Mungu ... aliwaumba." Mwanzo 1:27 . "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni." Mathayo 5:16 . "Nitakuja tena niwakaribishe Kwangu, ili nilipo Mimi, nanyi mwepo." Yohana 14:3 .

**Jibu:** Kwa sababu Biblia inajibu maswali ya kutatanisha maishani:
Nimetoka wapi? Mungu alituumba kwa mfano Wake. Hatukuibuka sisi kwa bahati mbaya kama globu au bonge fulani la maji na mada lisilo za kawaida au kutoka kwenye utelezi kama wa konokono eti ndiyo baadaye bonge hilo likaendelea na tukawa watu! Sisi ni wana na binti za Mungu, Mfalme Mwenye Nguvu Wagalatia 3:26 . Sisi ni wenye thamani sana kwa Mungu hivi kwamba Adamu na Hawa walipofanya dhambi, Mwenyezi Mungu alimtoa Mwana Wake afe na kulipa deni la dhambi zetu ili tuwe huru. YeyeAnataka kuturudisha kwa mfano Wake na kisha, upesi, kuturudisha kwenye Edeni mpya, makao ambayo Adamu na Hawa walipoteza.

Kwa nini niko hapa duniani? Malengo yetu ya maisha leo yanapaswa kuwa kugundua majibu ya ajabu ya Biblia kwa matatizo ya kutatanisha ya maisha na kukubali toleo la Yesu la kuturudisha kwenye mfano Wake Warumi 8:29 .

Je! ni nini kinatusubiri katika wakati ujao? Hakuna kubashiri juu ya siku zijazo. Yesu atakuja upesi sana kuwachukua watu Wake hadi kwenye makao ya fahari aliyowaandalia watu hukombinguni. Huko, watu wakiwa na shangwe na furaha nyingi, wataishi milele Yohana 14:1-3 Ufunuo 21:3 , 4 .

**13. Ninamshukuru Mungu kwa kunipa majibu chanya kwa maswali yenye kutatanisha maishani.**

**Jibu:**

**Maswali ya Kutafakari**

**1. Mimi ninaudhika kwamba Biblia inatoa maelezo hayo yenye kuchukiza na ya wazi ya dhambi katika kurekodi maisha ya baadhi ya watu wanaotajwa katika Biblia. Je, hii ni lazima kweli? Warumi 15:4**
Ndiyo. Ni mojawapo ya mambo makuu yanayoipa Biblia uaminifu. Wasifu mwingi huruka au kulainisha ubaya wa watu na mara nyingi huzidisha uzuri na kutia chumvi kuhusu yale mambo ambayo watu wameyafanya. Kutuambia mambo kama ilivyo huwapa watu imani kwamba Biblia inaweza kuaminiwa, kwani haifichi. Zaidi ya hayo, mbinu ya Shetani ni kuwaonyesha na kuwapa mkazo watu kuwa wao ni wadhambi wakubwa sana hivi kwamba Mungu hawezi au kuwaokoa. Ni shangwe iliyoje inayowakumba watu hao wanapoonyeshwa visa vya Biblia vya watu kama wao waovu na wabaya zaidi ambao Mungu aliwakomboa kutoka katika dhambi na kuwahesabia haki Warumi 15:4 !

**2. Je, Biblia yote imeongozwa na roho? Wengi wanaamini kuwa ni sehemu tu. 2 Timotheo 3:16**
Biblia ina jibu: "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki. 2 Timotheo 3:16 . Biblia haina Neno la Mungu tu ndani yake. Badala yake Ndiyo i Neno la Mungu. Biblia ni mwongozo wa habari na uendeshaji wa maisha ya mwanadamu. Puuza chochote chake na utakuwa na shida na taabu zisizo za lazima.

**3. Biblia ni kitabu cha kale chenye maneno na dhana za kizamani. Je, huoni kuwa si salama kutegemea kitu ambacho kimeondolewa mbali na siku zetu za kuelimika na usomi? 1 Petro 1:25**
Hapana. Umri wake uko katika upendeleo/manufaa Yake. Hiyo ni, kwa hakika, moja ya uthibitisho wa uvuvio wake. Biblia inasema, "Neno la Bwana hudumu hata milele." 1 Petro 1:25 . Biblia inasimama kama mwamba. Ni kitabu cha Mungu, Neno Lake Mwenyewe. Hakiwezi kuharibiwa. Wanadamu na hata mataifa yote yameichoma Biblia, wameipiga marufuku, na kujaribu kuidharau na hata kuiharibu Biblia, lakini badala yake, wamejidharau wenyewe. Wametoweka duniani, na mashambulizi yao dhidi ya Biblia yamesahauliwa. Bado Biblia inasalia kuwa kitabu kinachouzwa zaidi (best seller) kwa miaka maelfu, na kinachohitajika mara kwa mara kuliko kitabu kingne. Mamilioni wangekufa kwa ajili yake, ikiwa ni lazima. Ujumbe wake umetoka kwa Mungu na unaendana na maisha na matukio ya leo kwa asilimia 100 (up to date). Kabla ya kuisoma, Sali na umwombe Mungu afungue moyo wako unapoisoma.

**4. Baadhi ya watu mahiri zaidi ulimwenguni, ambao wamejifunza Biblia kwa makini, wanaamini hakuna anayeweza kuielewa. Ikiwa Biblia kweli ni kitabu cha Mungu, je, si kila mtu anaweza kuielewa?**
Watu wenye akili timamu wanaoweza kuelewa na kueleza karibu jambo lolote mara nyingi husimama au husita kwa haraka wanaposoma Biblia. Sababu ni kwamba mambo ya kiroho "yanatambulika kwa jinsi ya rohoni". 1 Wakorintho 2:13 , 14 . Mambo ya kina ya Neno hayataeleweka kamwe na akili ya kilimwengu, hata mtu awe na kipaji kiasi gani. Mtu asipotafuta uaminifu uzoefu na Mungu, hawezi kuelewa mambo ya Mungu. Roho Mtakatifu, Ndiye ambaye anafafanua Biblia Yohana 16:13 14:26 , Biblia haieleweki kwa akili ya kimwili, na ya kilimwengu. Kwa upande mwingine, Mkristo mnyenyekevu, hata asiye na elimu anayejifunza Biblia anapokea ufahamu wa ajabu kutoka kwa Roho Mtakatifu Mathayo 11:25 1 Wakorintho 2:9 , 10 .

**5. Biblia imejaa makosa. Unawezaje kuamini kuwa imevuviwa? Isaya 28:9**
Mengi sana ya yale yanayoitwa makosa katika Biblia yameonyeshwa kuwa makosa ya uamuzi au ukosefu wa uelewaji kwa upande wa wale wanaolalamika. Haya sio makosa hata kidogo, ila Ukweli haueleweki. Biblia iliyovuviwa:
Siku zote itakuambia Ukweli.
Haitakupotosha kamwe.
Inaweza kuaminiwa kikamilifu.

Ni yenye kutegemeka na yenye mamlaka, si tu katika mambo ya kiroho bali pia katika mambo mengine ambayo inazungumzia, Hutia ndani historia na sayansi.
Sikuzote Shetani anachimbua dosari fulani katika Maandiko, jambo ambalo halishangazi. Alipata kosa hata kwa Mungu mbinguni. Huenda walionakili walifanya makosa katika visa fulani, lakini hakuna kinachofikiriwa kilichotendeka au kosa lingine lolote linalodaiwa kuathiri Ukweli wa Neno la Mungu. Fundisho la Biblia halijajengwa juu ya Fungu moja tu la Biblia, bali juu ya jumla ya maoni ya Mungu juu ya somo lolote. Hatujui makosa yoyote yanayodaiwa ya aina yoyote ambayo yangeathiri Ukweli wa maudhui ya Maandiko. Baadhi ya mambo katika Maandiko bado ni magumu kuyapatanisha. Daima kutakuwa na nafasi ya shaka kwa wale wanaopendelea kuwa na shaka. Tunaamini kwamba hata makosa yanayodaiwa yako, na ambayo bado hayajaelezewa kikamilifu, kama ilivyokuwa awali, haya yatafichuliwa hivi karibuni kama kengele za uongo. Kadiri watu wanavyojitahidi kuidhoofisha Biblia, ndivyo nuru yake inavyozidi kuangaza. Imechomwa, imefukiwa, imezikwa kwenye udongo, na imepigwa marufuku lakini bado ndiyo kitabu kinachouzika kwa wingi kuliko kitabu chochote duniani toka ianze kunakiliwa na mkono. Mwaka 1456 Johannes Gutenberg alivumbua mtambo wa kuchapa na Biblia ya kwanza ilianzwa kuchapwa kwa mashine kule Ujerumani, na mpaka leo. Kitabu cha Mwisho cha Ufunuo tunapokisoma, kinasema upande wa Mungu unashinda, japo tunaona kama mara zingine adui anashinda, turudi kitabu cha Ufunuo 1:3 ambayo inasema "Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu."
Soma, Sikia na Shika, Kitabu hiki!

## Maswali ya Maswali

**1. Ni unabii gani uliotimizwa unaothibitisha kwamba Biblia ilipuliziwa? (4)**
_____ Koreshi angeiteka Babeli
_____ Ronald Reagan angekuwa rais wa Marekani.
_____ Misri haingekuwa tena taifa lenye nguvu na linaloongoza.
_____ Maadili yangezorota katika siku za mwisho.
_____ Ujerumani ingekuwa na ukame wa miaka 20.
_____ Babeli, ilipoharibiwa, haikukaliwa tena.

**2. Yesu alionyesha imani yake katika uvuvio wa Biblia kwa:**
_____ Kuzungumza kwa sauti juu ya somo.
_____ Akinukuu kutoka kwayo alipokuwa akifundisha.
_______Kuwashushia moto wenye shaka.
_____ Akitangaza kutoka kwenye ngazi za hekalu.

**3. Biblia inataja mambo gani ya kisayansi kutoka kwenye orodha iliyo hapa chini? (3)**
_____ Dunia ni duara.
_____ Hewa ina uzito.
_____ Mungu huzuia atomi kuruka mbali.
_____ Fomula ya maji ni ‘H2O’.
_____ Maji ya bahari yana chumvi.

**4. Ni ipi kati ya sheria zifuatazo za afya zinazopatikana katika Biblia? (2)**
_____ Kunywa lita nne za maji kila siku.
_____ Acha vileo.
_____ Endesha kila asubuhi na usiku.
_____ Epuka mwenendo mpotovu wa ngono.

**5. Maneno yafuatayo kuhusu Biblia ni ya Kweli: (3)**
_____ Takriban watu 40 walisaidia kuandika Biblia.
_____ Biblia iliandikwa kwa muda wa miaka 10,000.
_____ Sehemu za Biblia pekee ndizo zimevuviwa.
_____ Mwandishi halisi wa Biblia ni Roho Mtakatifu.
_____ Biblia inauzwa sana (Best Seller ya miaka yote).

**6. Ni yapi kati ya yafuatayo ambayo Biblia ilitabiri kuhusu maisha ya Masihi? (3)**
_____ Angezaliwa Nazareti.
_____ Angeruka mbinguni mara kwa mara.
_____ Angeuzwa kwa vipande 30 vya fedha.
_____ Herode angejaribu kumuua.
_____ Angesulubishwa.
_____ Atafufuliwa baada ya miaka saba.

**7. Ni kanuni gani ya Biblia, ikifuatwa, ingeweza kuzuia UKIMWI vyema zaidi?**
_____ Usiwe mzinzi.
_____ Usiabudu sanamu za kuchonga.
_____ Kula chakula mara kwa mara.

**8. Ni kauli gani hapa chini ni za kweli kuhusu uibukaji? (3)**
_____ Ni nadharia ambayo haijathibitishwa.
_____ Inadhoofisha Ukristo.
_____ Ni ukweli uliothibitishwa.
_____ Inathibitisha kwamba wanadamu na nyani wana mababu wa pamoja.
_____ Ni itikadi kali ya ukomunisti.

**9. Ni maneno gani hapa chini yanasaidia kuthibitisha kwamba Biblia ilivuviwa**
_____ Wasifu wake unajumuisha wabaya na wazuri pia.
_____ Inabadilisha maisha ya wafuasi wake.
_____ Unabii wa Agano la Kale kuhusu Masihi ulitimizwa na Yesu.
_____ Ilitabiri kuinuka kwa falme nne za ulimwengu.
_____ Umoja wake.
_____ Inasimulia siku na saa ya ujio wa pili wa Yesu.

**10. Mungu aliumba dunia katika siku sita halisi za saa 24.**

_____
Kweli _____ Si kweli

**11. Katika siku za Nuhu, gharika ya ulimwenguni pote iliharibu kila kitu kilicho hai isipokuwa viumbe vya baharini na vile vilivyokuwa ndani ya safina.**

_____
Kweli _____ Si kweli

**12. Lugha mbalimbali za ulimwengu zilianzia kwenye Mnara wa Babeli.**

_____
Kweli _____ Si kweli

**Je, Mungu Alimuumba Shetani**

**Somo la 2**

Watu wengi ulimwenguni wanadanganywa na fikra za mwovu aliye na nia ya kuharibu maisha yao – mpangaji mikakati mahiri anayeitwa ibilisi, au Shetani. Lakini huyu mkuu wa giza ni zaidi ya vile unavyoweza kufikiri...wengi husema ni kiumbe aliyebuniwa na ni uzushi tu, kwamba yeye si halisi, lakini Biblia inasema yeye ni halisi kabisa, na anadanganya familia, makanisa, na hata mataifa ili kuongeza huzuni na maumivu. Hapa kuna mambo ya ajabu ya Biblia kuhusu mkuu huyu wa giza na jinsi unavyoweza kumshinda!

Dhambi ilitokana na Shetani, ambaye pia anaitwa Ibilisi.

**1. Dhambi ilianzia na nani?**

"Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo." 1 Yohana 3:8 . "Yule nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi, na Shetani." Ufunuo 12:9 .

**Jibu:** Shetani, ambaye pia anaitwa ibilisi, ndiye mwanzilishi wa dhambi. Bila Maandiko, chanzo cha uovu kingebaki bila kufafanuliwa.

Shetani alikuwa akiishi mbinguni alipofanya dhambi. Jina lake lilikuwa Lusifa, ambayo iinamaanisha "Nyota ya Siku."

**2. Shetani aliitwa nani kabla ya kutenda dhambi? Alikuwa akiishi wapi wakati huo?**

"Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ee Lusifa, mwana wa asubuhi!" Isaya 14:12 . Yesu alisema, "Nilimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama umeme." Luka 10:18 . "Ulikuwa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu." Ezekieli 28:14 .

**Jibu:** Jina lake lilikuwa Lusifa, na alikuwa akiishi mbinguni. Lusifa anafananishwa na mfalme wa Babeli katika Isaya 14 na kama mfalme wa Tiro katika Ezekieli 28.

Lusifa alikuwa malaika wa mbinguni aliyeumbwa na Mungu. Alikuwa mkamilifu katika hekima na uzuri na alisimama karibu na kiti cha enzi cha Mungu.

**3. Asili ya Lusifa ilikuwa nini? Alikuwa na wadhifa gani? Biblia inamfafanuaje?**

"Wewe uliumbwa." Ezekieli 28:13 , 15 . "Wewe ndiwe kerubi aliyetiwa mafuta afunikaye." Ezekieli 28:14 . "Uliitia muhuri jumla, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako; kazi ya matari yako na filimbi zako ilitengenezwa ndani yako siku ile uliyoumbwa. . Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako." Ezekieli 28:12-15 .

**Jibu:** Lusifa *aliumbwa* na Mungu, kama vile malaika wengine wote (Waefeso 3:9 ). Lusifa alikuwa kerubi "afunikaye" au malaika. Malaika mmoja mkuu anasimama upande wa kushoto wa kiti cha enzi cha Mungu na mwingine upande wa kuume ( Zaburi 99:1 ). Lusifa alikuwa mmoja wa wale viongozi wa malaika walioinuliwa sana. Uzuri wa Lusifa haukuwa na dosari na wa kuvutia. Hekima yake ilikuwa kamilifu. Mwangaza wake ulikuwa wa kutisha. Andiko la Ezekieli 28:13 laonekana kuonyesha kwamba koo lake lilitayarishwa rasmi ili kumfanya awe mwanamuziki mahiri. Wengine wanafikiri aliongoza kwaya ya malaika.

Shetani anataka watu wamwabudu. Hata alijaribu kumshawishi Yesu amwabudu.

**4. Ni nini kilitokea katika maisha ya Lusifa ambacho kilimfanya atende dhambi? Ni dhambi gani ya kufuru aliyoifanya hatimaye?**

"Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako, umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako." Ezekieli 28:17. "Kwa maana umesema moyoni mwako, ... Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu: ... nitafanana na Yeye Aliye juu." Isaya 14:13 , 14 .

**Jibu:** Kiburi, wivu, kutoridhika, na kujikweza kuliibuka katika maisha yake. Lusifa aliamua kujaribu kumwangusha Mungu na kisha kuwataka wote wamwabudu. Ulikuwa ni uhaini wa aina mbaya zaidi.

**Kumbuka:** Kwa nini ibada ni jambo kubwa? Kuabudu ni jambo la msingi katika vita vinavyoendelea kati ya Mungu na Shetani. Watu waliumbwa wawe na furaha na kuridhika pale tu wanapomwabudu Mungu pekee. Hata malaika wa mbinguni wasioanguka hawapaswi kuabudiwa ( Ufunuo 22:8 , 9 ). Shetani alitafuta kuabudiwa hapo mwanzo. Karne nyingi baadaye, alipomjaribu Yesu nyikani, ibada bado ilikuwa suala kuu ( Mathayo 4:8-11 ). Katika siku hizi za mwisho, Mungu anawaita watu wote kumwabudu ( Ufunuo 14:6 , 7 ). Hili linamkasirisha Shetani sana hivi kwamba atajaribu kuwalazimisha watu kumwabudu ama sivyo wauawe ( Ufunuo 13:15 ).

Kila mtu anaabudu mtu au kitu Fulani, hakuna aliye katikati, baadhi ya vitu vinavyoabudiwa: mamlaka, heshima, watoto, mume, kabila, uzuri, kisomo, chakula, anasa, mali, maoni ya mtu mwenyewe, nk Mungu anasema, "Usiwe na miungu mingine ila Mimi." Kutoka 20:3 . Na tusipomwabudu Yeye peke yake, anatuhesabu dhidi Yake ( Mathayo 12:30 ). Habari hii inashangaza, lakini ni kweli. Ikiwa kitu chochote au mtu mwingine yeyote isipokuwa Mungu anapata nafasi ya kwanza katika maisha yangu, labda mimi ninamwabudu na kumuunga mkono Shetani bila kujua masikini. Je, Mungu ana nafasi ya kwanza maishani mwangu, au je, ninamwinua Shetani bila kufahamu? Ni swali gumu, au sivyo?

Kutoridhika kwa Lusifa kukawa uasi wa wazi dhidi ya Mungu. Theluthi moja ya malaika wa mbinguni walijiunga naye katika jaribio la kumpindua Mungu. Matokeo yake, Lusifa na wafuasi wake walitupwa kutoka mbinguni.

**5. Ni nini kilitokea mbinguni kama tokeo la uasi wa Lusifa?**

"Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani. , aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye." Ufunuo 12:7-9 .

**Jibu:** Lusifa alipata msaada wa theluthi moja ya malaika ( Ufunuo 12:3 , 4 ) na kusababisha uasi mbinguni. Mungu hakuwa na chaguo ila kumfukuza Lusifa na malaika zake. Hii ilikuwa ni vita kubwa zaidi, kuwahi kupiganwa. Kusudi la Lusifa lilikuwa kunyakua kiti cha enzi cha Mungu, hata ikiwa hatimaye inaweza kusababisha mauaji ( Yohana 8:44 ). Baada ya kufukuzwa kwake kutoka mbinguni, Lusifa aliitwa Shetani (adui) na ibilisi (mchongezi), na malaika zake waliitwa mashetani.

Makao makuu ya Shetani ni dunia. Anawachukia wanadamu na analenga kumuumiza Mungu kwa kukuangamiza.

**6. Makao makuu ya Shetani ya sasa yako wapi? Anahisije kuhusu watu?**

"Bwana akamwambia Shetani, Umetoka wapi wewe? Ayubu 2:2 . "Ole wa nchi na bahari, kwa maana Ibilisi ameshuka kwenu mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu." Ufunuo 12:12 . "Adui yenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze." 1 Petro 5:8 .

**Jibu:** Kinyume na maoni ya watu wengi, makao makuu ya Shetani ni dunia, si moto wa mateso. Mungu aliwapa Adamu na Hawa mamlaka juu ya dunia ( Mwanzo 1:26 ). Walipotenda dhambi, walipoteza utawala wao kwa Shetani ( Warumi 6:16 ), ambaye kisha akawa mtawala, au mkuu, wa dunia ( Yohana 12:31 ). Shetani anawachukia sana wanadamu ambao waliumbwa kwa mfano wa Mungu. Hawezi kumgusa Mungu. Kwa hiyo, badala yake, sumu yake inaelekezwa dhidi ya watu ambao ni watoto wa Mungu. Yeye ni muuaji mwenye chuki, mkatili ambaye lengo lake ni kukuangamiza na hivyo kumuumiza Mungu.

Adamu na Hawa hawakupaswa kula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya, chini ya adhabu ya kifo.

**7. Mungu alipowaumba Adamu na Hawa, ni jambo gani moja alilokataza wasifanye? Je, adhabu ya kutotii ilikuwa ipi?**

"Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika." Mwanzo 2:17 .

**Jibu:** Hawakupaswa kula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Adhabu ya kula mti huo ilikuwa kifo.

Shetani alichukua umbo la nyoka anayezungumza na kumshawishi Hawa kula tunda lililokatazwa.

**8. Shetani alitumia mtu gani kumdanganya Hawa? Shetani alimwambia uwongo gani?**

"Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Naam, ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya *kila* mti wa bustani?" "Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa; kwa maana Mungu anajua ya kuwa siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama miungu, mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:1 , 4 , 5 , mkazo umeongezwa.

**Jibu:** Shetani alimtumia nyoka—mnyama mwenye hekima zaidi na mwenye kuvutia zaidi kati ya wale Mungu aliumba—ili kumdanganya Hawa. Wengine wanafikiri hapo awali nyoka alikuwa na mbawa na akaruka (Isaya 14:29 ; 30:6 ). Kumbuka, hakutambaa hadi Mungu alipomlaani (Mwanzo 3:14 ). Uongo wa Shetani ulikuwa: (1) hutakufa, na (2) kula tunda kutakufanya uwe na hekima. Shetani, aliyebuni uwongo ( Yohana 8:44 ), alichanganya Ukweli na uwongo aliomwambia Hawa. Uongo unaojumuisha Ukweli fulani ndio udanganyao kuliko yote. Ingekuwa ni Kweli "wangejua ubaya" baada ya kutenda dhambi. Kwa upendo, Mungu alikuwa amewanyima ujuzi wa huzuni, masikitiko, mateso, maumivu, na kifo. Shetani, kama anavyofanya leo, ndivyo alifanya wakati huo kwamba ujuzi wa uovu uonekane wenye kuvutia.

Shetani alisema uwongo ili kupotosha tabia ya Mungu kwa sababu alijua kwamba hakuna mtu ambaye angemwacha Mungu Mwenye upendo kama huyo isipokuwa asielewe tabia Yake.

Kula tunda lililokatazwa kulifanya Adamu na Hawa kushirikiana na Shetani, adui mkali wa Mungu.

**9. Je, kula kipande cha tunda lilikuwa jambo baya sana? Kwa nini Adamu na Hawa waliondolewa kwenye bustani?**

"Kwake yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi." Yakobo 4:17 . "Dhambi ni uvunjaji wa sheria." 1 Yohana 3:4 . "Atendaye dhambi ni wa Ibilisi." 1 Yohana 3:8 . "Bwana Mungu akasema, Tazama, mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asije akanyosha mkono wake, akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele. ." "Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima." Mwanzo 3:22 , 24 .

**Jibu:** Ndiyo, kula tunda lilikuwa dhambi kwa sababu ilikuwa ni kukataa moja kwa moja mojawapo ya matakwa machache ya Mungu. Ilikuwa ni uasi wa wazi dhidi ya sheria na mamlaka ya Mungu. Kwa kukataa mojawapo ya amri za Mungu, Adamu na Hawa walishirikiana na Shetani, adui wa Mungu, na hivyo kuleta utengano kati yao wenyewe na Mungu ( Isaya 59:2 ). Shetani alitumaini kwamba wanandoa wangetenda dhambi na kisha kula matunda ya mti wa uzima, na hivyo kuwa wenye dhambi wasioweza kufa. Lakini Mungu aliwaondoa kwenye bustani ili kuzuia janga kama hilo.

**10. Biblia inafunua mambo gani yenye kustaajabisha kuhusu mbinu za Shetani za kuumiza, kuwadanganya, kuwavunja moyo, na kuwaangamiza watu?**

**Jibu:** Shetani hutumia kila njia inayoweza kufikiwa ili kuwadanganya na kuwaangamiza watu. Mashetani/mapepo wake wanaweza kuonekana na kujifanya kuwa watu waadilifu, au hata viongozi wa dini. Na Shetani atatokea kama malaika wa utukufu wa nuru na uwezo wa kuita moto kutoka mbinguni. Atajifanya kuwa Yesu. Lakini wewe umeonywa, kwa hivyo usikubali. Yesu atakapokuja, *kila jicho litamwona* ( Ufunuo 1:7 ). Atakaa mawinguni na asiiguse nchi, hivyo ukisikia Yesu Yupo Mwanza, au Kigali au Goma usiamini! ( 1 Wathesalonike 4:17 ).

| **Biblia inasema Shetani:** | |
|---|---|
| Hudanganya/hutesa (Ufunuo 12:9, 13) | Nukuu zisizo sahihi katika Biblia (Mathayo 4:5 , 6 ) |
| Mashtaka ya uwongo / mauaji (Ufunuo 12:10 Yohana 8:44 ) | Mitego/ nyavu( 2 Timotheo 2:26 1 Petro 5:8 ) |
| Hufanya vita dhidi ya watu wa Mungu ( Ufunuo 12:17 ) | Hufunga/huchochea usaliti ( Luka 13:16 Yohana 13:2 , 21 ) |
| Wafungwa ( Ufunuo 2:10 ) | Mali/vizuizi ( Luka 22:3-5 1 Wathesalonike 2:18 ) |
| Hufanya miujiza/uongo ( Ufunuo 16:13 , 14 Yohana 8:44 ) | Anaonekana kama malaika wa nuru (2 Wakorintho 11:13-15 ) . |
| Huleta magonjwa / mateso (Ayubu 2:7) | Pepo wake hujifanya kuwa wachungaji ( 2 Wakorintho 11:13-15 ) . |
| Kashfa ("Ibilisi" maana yake "mchongezi") | Anaita moto kutoka mbinguni (Ufunuo 13:13 ) |

Nguvu za udanganyifu za wakati wa mwisho za Shetani zitakuwa kubwa sana hivi kwamba karibu ulimwengu wote utamfuata.

**11. Majaribu na mbinu za Shetani vina nguvu na matokeo ya kadiri gani?**

Alisadikisha: thuluthi moja ya malaika ( Ufunuo 12:3-9 ); Adamu na Hawa (Mwanzo 3); wote isipokuwa watu wanane katika siku za Nuhu ( 1 Petro 3:20 ). Atafanya waliopotea wajisikie wameokolewa ( Mathayo 7:21-23 ). Karibu ulimwengu wote utamfuata ( Ufunuo 13:3 ). Wachache wataokolewa ( Mathayo 7:14 ; 22:14 ).

**Jibu:** Kiwango cha mafanikio cha Shetani ni cha juu sana hivi kwamba kinaonekana kuwa kisichoaminika. Akawadanganya theluthi *moja ya malaika* . Katika siku za

Nuhu, *wote isipokuwa watu wanane* walidanganywa. Kabla ya Yesu kuja mara ya pili, Shetani atatokea kama malaika, akijifanya kuwa Kristo. Nguvu yake ya udanganyifu itakuwa kubwa sana kwamba *usalama wetu pekee utakuwa katika kukataa kwenda kumwona* ( Mathayo 24:23-26 ). Ukikataa kabisa kutazama na kusikiliza, Yesu atakulinda na udanganyifu ( Yohana 10:29 ).

Mwishoni mwa ulimwengu, Shetani atatupwa ndani ya ziwa la moto, ambalo litamgeuza kuwa majivu na kukomesha kuwapo kwake milele.

**12. Ibilisi atapata adhabu yake lini na wapi? Je, adhabu hiyo itakuwa nini?**

"Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia hii. Mwana wa Adamu atawatuma malaika Zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme Wake machukizo yote, na watenda maovu, na kuwatupa katika tanuru ya moto. ." Mathayo 13:40-42 .

"Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika lile ziwa la moto na kiberiti." Ufunuo 20:10 . "Ondokeni Kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake. Mathayo 25:41 . "Kwa hiyo nitatokeza moto kutoka kati yako, nao utakuteketeza, Nami nitakufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao ... wala hutakuwapo tena kamwe. Ezekieli 28:18 , 19 .

**Jibu:** Ibilisi atatupwa katika ziwa la moto juu ya dunia hii katika mwisho wa dunia. Moto utamla Shetani, utamgeuza kuwa majivu, na kukomesha kuwepo kwake milele. Moto huu pia utawaangamiza wenye dhambi wote. Katika onyesho hili la mwisho, hakuna hata mmoja aliye upande wa Mungu atakayekufa na hakuna hata mmoja aliye upande wa Shetani atakayeokoka. ***Kumbuka:*** *Haiwezekani kueleza vya kutosha huzuni na uchungu ambao Baba na Mwana watapata wakati wa uharibifu wa Shetani. Alikuwa karibu nao zaidi kuliko kiumbe mwingine yeyote—rafiki mchangamfu na wa kibinafsi. Kumwangamiza yeye na mamilioni ya watu waliomfuata kutawaumiza Baba na Mwana zaidi kuliko kuungua kutakavyoumiza mtu yeyote katika moto.*

Watu wa Mungu mbinguni watakuwa salama kutoka kwa dhambi milele. Haitafufuka tena.

**13. Je, ni nini kinachotatua milele tatizo la kutisha la dhambi? Je, dhambi itatokea tena?**

"Kama niishivyo, asema Bwana, kila goti litapigwa mbele zangu, na kila ulimi utakiri kwa Mungu." Warumi 14:11 . (Ona pia Wafilipi 2:10 , 11 ; Isaya 45:23 .) "Mateso hayatainuka mara ya pili; Nahumu 1:9 .

**Jibu:** Matukio mawili muhimu yatatua tatizo la dhambi:

**Kwanza** , viumbe vyote mbinguni na duniani, ikiwa ni pamoja na shetani na malaika zake, kwa hiari yao wenyewe watapiga magoti na kukiri hadharani kwamba Mungu ni mkweli, Mwenye haki, na mwadilifu. Hakuna maswali yatakayobaki bila majibu. Watenda-dhambi wote watakiri waziwazi kwamba wamepotea kwa sababu ya

kukataa kwao kwa dhamira safi kuukubali upendo na wokovu wa Mungu. Watakubali kwamba haki inadai lazima wafe. Wote watakiri kwamba wanastahili kifo cha milele.

**Pili** , dhambi itasafishwa kutoka kwa ulimwengu kwa uharibifu kamili na wa mwisho wa dhambi, wenye dhambi, shetani na malaika zake. Mungu ana maoni chanya kuhusu jambo hili: Dhambi haitatokea tena ili kuharibu ulimwengu wa Mungu- Nahum 1:9.

Yesu alifanya uharibifu wa dhambi uwezekane.

**14. Ni nani anayefanya uondoaji wa mwisho na kamili wa dhambi kutoka kwa ulimwengu kuwa hakika?**

"Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi." 1 Yohana 3:8 . "Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na nyama, Yeye Naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa mauti amharibu yeye aliyekuwa na guvu za mauti, yaani, Ibilisi." Waebrania 2:14 .

**Jibu:** Kupitia maisha Yake, kifo, na ufufuo Wake, *Yesu* alifanya kuondolewa kwa dhambi kuwa hakika.

Mungu, Baba yetu, anatupenda zaidi kuliko baba yeyote wa kidunia angeweza kuwapenda watoto Wake. Hawezi kusubiri kutupokea katika ufalme Wake mpya.

**15. Mungu Baba anahisije kuhusu watu?**

"Baba Mwenyewe anawapenda ninyi." Yohana 16:27 . (Ona pia Yohana 3:16 ; 17:22 , 23 .)

**Jibu:** Baba anawapenda watu kama vile Mwana anavyowapenda. Lengo kuu la Yesu maishani lilikuwa kuonyesha tabia ya Baba Yake katika maisha Yake ili watu wajue jinsi Baba alivyo Mwenye upendo, mchangamfu na anayejali (Yohana 5:19 ).

**Shetani Anamwakilisha Baba Vibaya**

Shetani anamwakilisha Baba vibaya kama *asiye na hisia, asiye na kujali, asiye na upendo, mnyanyasaji, mkali, na asiyeweza kufikiwa* (tabia za shetani mwenyewe anambambika Mungu). Hata anataja matendo yake mwenyewe mabaya, yenye kuleta msiba kuwa "matendo ya Mungu." na hii inaonekana kwenye bima, watu husema 'act of God' walato wa maafa kama mafuriko au radi. Yesu alikuja kufuta kashfa hii kutoka kwa Jina la Baba Yake na kuonyesha kwamba Baba yetu wa mbinguni anatupenda zaidi kuliko mama anavyompenda mtoto wake ( Isaya 49:15 ). Mada kuu ya Yesu aliyoipenda sana kilikuwa subira, huruma, na rehema nyingi za Mungu.

**Baba Hawezi Kungoja Kwa Shida**

Ili kuwafanya watu wawe na furaha ya hali ya juu, Baba yetu wa mbinguni amewaandalia makao mazuri ya milele. Ndoto zetu hapa hazilingani na kile

ambacho kinatungoja huko! Ni vigumu Kwake kungoja kuwakaribisha watu Wake kwenye ile siku ya furaha ya kurudi nyumbani iliyo mbele tu. Hebu tupate neon hili na kauli mbiu hii! Hebu na tuwe tayari. Muda uliosalia tayari umeanza.

**16. Ninafurahi kujua kwamba Mungu Baba ananipenda kama Yesu anavyonipenda.**

**Jibu:**

# MASWALI YA KUCHEUA

**1. Je, tunda ambalo Adamu na Hawa walikula lilikuwa tufaha/apple?**

Hatujui. Biblia haisemi.

**2. Dhana ambayo inamwonyesha shetani kama mnyama mwekundu, nusu-mtu na nusu-nusu mwenye pembe na mkia ilianzia wapi?** Ilitoka katika hadithi za kipagani na inampendeza shetani. Shetani Anajua watu wanaofikiri wanakataa mazimwi kama hadithi za uongo wataongozwa kukataa kuwepo kwake. Wale wasiomwamini shetani ndio huwa wa kwanza kunaswa na hila zake.

**3. Mungu akawaambia Adamu na Hawa, Siku utakapokula matunda ya mti huo, utakufa hakika. Mwanzo 2:17. Kwa nini hawakufa siku hiyo?**

Biblia inazungumza juu ya vifo viwili:
(1) Kifo cha "kwanza" sisi sote tunakufa ( Waebrania 9:27 ).
(2) Kifo cha "pili" ambacho waovu hufa katika moto wa mateso mwishoni mwa wakati ( Ufunuo 21:8 ).
Tofauti ni kwamba hakuna ufufuo kutoka katika kifo cha pili. Ni ya milele.

**Yesu Alikufa Kifo cha Pili kwa Kila Mtu**

Wakati Adamu na Hawa walipofanya dhambi, mara moja wangekufa kifo cha pili isipokuwa kwa ule Ukweli kwamba Yesu alisonga mbele na kutoa kifo cha pili cha Kalvari kwa kila mtu. Dhabihu Yake kuu iliwaepusha ( Waebrania 2:9 ).

**Adamu Alipofanya Dhambi, Asili Yake "Isiyokufa" Ikawa Asili "Inayokufa"**
Kuhusu kifo cha kwanza, tafsiri halisi ya neno "kufa" katika Mwanzo 2:17 ni "kufa utakufa," ambayo imetajwa kwenye ukingo wa wengi. Biblia. Inamaanisha kwamba Adamu na Hawa wangeingia katika mchakato wa kufa. Kabla ya kutenda dhambi, wenzi hawa walikuwa na asili isiyokufa, isiyo na dhambi. Asili hii ilidumishwa kwa kula matunda ya mti wa uzima. Wakati wa dhambi, asili zao zilibadilika hadi kufa, kwaajili ya asili ya dhambi. Hivi ndivyo Mungu alivyotabiri. Kwa sababu walizuiliwa kutoka kwa mti wa uzima, matokeo ya dhambi kama kuoza, kuharibika, na kuwepo kifo, kulianza mara moja. Kaburi likawa la uhakika. Bwana alisisitiza hili baadaye alipowaambia, "Kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi." Mwanzo 3:19 .

**4. Lakini kwa kuwa Mungu alimuumba Lusifa, je, si kweli anawajibika kwa dhambi yake?**

Hapana kabisa. Mungu alimuumba Lusifa malaika mkamilifu, asiye na dhambi. Lusifa alijifanya shetani kwa uchaguzi wake. Uhuru wa kuchagua ni kanuni ya msingi ya serikali ya Mungu. Mungu alijua Lusifa angetenda dhambi wakati alipomuumba. Ikiwa wakati huo Mungu angalikataa kumuumba, Angekuwa akiikataa kanuni hiyo kuu ya uhuru wa kuchagua.

**“Uhuru wa Kuchagua” ni Njia ya Mungu**

Kwa hiyo, akijua vizuri kile Lusifa angefanya, na bado Mungu alimuumba. Mambo hayohayo yanahusu uumbaji wa Adamu na Hawa. Na, karibu na nyumbani, Ukweli huu unatumika kwako na mimi. Mungu anajua kabla hatujazaliwa jinsi tutakavyoishi, lakini hata hivyo, anaturuhusu tuishi na kuchagua kuidhinisha serikali yake au ya Shetani. Mungu Yuko tayari kueleweka vibaya na kulaumiwa kwa uwongo na kushutumiwa kwa miaka mingi, huku akichukua wakati kuruhusu kila mtu kuchagua kwa uhuru ambaye atamfuata.

**Ni Mungu Mwenye Upendo Pekee Ndiye Awezaye Kuhatarisha Kutoa Uhuru Kamili kwa Wote**

Zawadi hii tukufu na muhimu ya uhuru wa kuchagua inaweza tu kutoka kwa Mungu Mwenye haki, aliye wazi na Mwenye upendo. Ni heshima na furaha kumtumikia Bwana na rafiki kama huyo.

**Chagua Kumtumikia Mungu**

Tatizo la dhambi litakwisha hivi karibuni. Mwanzoni, kila kitu kilikuwa Kizuri sana.” Mwanzo 1:31 . Sasa “ulimwengu wote unakaa katika uovu.” 1 Yohana 5:19 . Watu kila mahali wanachagua kumtumikia Mungu au Shetani. Tumia uhuru *wako* wa ajabu, uliopewa na Mungu kuchagua kumtumikia Bwana.

**5. Kwa nini Mungu hakumwangamiza shetani alipotenda dhambi, na hivyo kumaliza tatizo la dhambi?**

Kwa sababu dhambi ilikuwa kitu kipya kabisa katika ulimwengu wa Mungu, na wakaaji wake hawakuielewa. Pengine hata Lusifa mwenyewe hakuielewa kabisa mwanzoni. Lusifa alikuwa kiongozi wa malaika mwenye kipaji, aliyeheshimika sana. Njia yake bila shaka ilikuwa ya kujali mbingu na malaika. Inawezekana ilifikiri kitu kama hiki: “Mbingu ni nzuri, lakini ingeboreshwa kwa pembejeo zaidi za malaika. Mamlaka nyingi sana zisizopingwa (kama Baba na Mwana wanavyo) huelekea kuwapofusha viongozi kwa maisha halisi. Malaika hawapaswi kutakiwa kuchukua maagizo. Tunapaswa kutoa amri. Mungu anajua mapendekezo yangu ni sahihi, na anahisi kutishwa.Tusiwaruhusu viongozi wetu watukufu ambao wametoka nje kuhatarisha uwepo wa mbingu. Watasikiliza ikiwa tutaenda kwa umoja. tusiwe dhaifu lazima tuchukue hatua. Vinginevyo, sote tutaharibiwa na serikali isiyotuthamini.”

**Theluthi moja ya Malaika Walijiunga na Lusifa**

Lusifa aliwasilisha hoja ambazo zilishawishi malaika wengi, na theluthi moja walijiunga naye. Ikiwa Mungu angemwangamiza Lusifa mara moja, baadhi ya viumbe kama malaika ambao hawakuelewa kabisa tabia ya Mungu wangeweza kuanza kumwabudu Mungu kwa hofu, wakisema, “Huenda Lusifa alikuwa sahihi. Kuwa mwangalifu. Ikiwa unatofautiana na Mungu, anaweza kukuua.” Kwa hivyo hakuna kitu ambacho kingetatuliwa. Badala yake, tatizo lingeongezeka.

**Mungu Hukubali Utumishi wa Upendo Pekee, wa Kujitolea**
Huduma pekee inayokubalika kwa Mungu ni huduma ya uchangamfu, ya kujitolea na inayochochewa na upendo. Utii kwa sababu nyingine yoyote haukubaliki.

**Je, Kumpa Shetani Wakati wa Kuonyesha Kanuni Zake Mungu**
Shetani alidai kwamba alikuwa na mpango bora zaidi kwa ajili ya serikali ya ulimwengu. Mungu amempa muda wa kuonyesha kanuni zake. Bwana atakomesha dhambi baada ya kila nafsi katika ulimwengu kusadikishwa kwamba serikali ya Shetani haina haki, ina chuki, haina huruma, inadanganya na inaharibu.

**Malimwengu yote na sayari zingine zinautazama Ulimwengu Huu**
Biblia inasema, “Tumefanywa kuwa tamasha kwa ulimwengu, na kwa malaika, na kwa wanadamu.” 1 Wakorintho 4:9 . Ulimwengu mzima unatazama kila mmoja wetu anaposhiriki katika pambano kati ya Kristo na Shetani. Pambano hilo likiisha, kila nafsi itaelewa kikamilifu kanuni za falme zote mbili na itakuwa imechagua kumfuata Kristo au Shetani. Wale ambao wamechagua kushirikiana na dhambi na Shetani wataharibiwa pamoja naye, na watu wa Mungu watachukuliwa hadi kwenye usalama wa milele wa makao yao ya mbinguni.

# MASWALI YA CHEMSHA BONGO KWIZZ

**1. Dhambi ilianza na nani? (1)**
_____ Mikaeli.
_____ Lusifa.
_____ Gabriel.

**2. Lusifa alikuwa akiishi wapi alipotenda dhambi mara ya kwanza? (1)**
_____ Duniani.
_____ Mbinguni.
_____ Kwenye Nyota ya Kaskazini.

**3. Angalia vitu vilivyowahi kumuelezea Lusifa: (6)**
_____ Malaika aliyeumbwa.
_____ Amejaa hekima.
_____ Alipanda farasi mweupe wa mbinguni.
_____ Mkamilifu katika njia zake.
_____ Mlinzi wa lango la mbinguni.
_____ Mwanamuziki bora.
_____ Mkamilifu kwa uzuri.
_____ Kerubi anayefunika.

**4. Weka alama kwenye vitu vinavyosema Ukweli kuhusu uasi wa Lusifa: (5)**

_____ Alitupwa kutoka mbinguni.
_____ Alitubu na kukaa mbinguni.
_____ Alijificha ndani ya jumba la kifalme.
_____ Jina lake likawa Shetani.
_____ Alikuwa mwenye dhambi wa kwanza.
_____ Yesu alimwona akitolewa nje.
_____ Theluthi moja ya malaika walianguka pamoja naye.

**5. Lusifa alitaka nini? (2)**
_____ Kuabudiwa.
_____ Kumwangusha Mungu na kuchukua nafasi Yake.
_____ Kuruka katika ulimwengu mzima.

**6. Angalia vitu ambavyo ni vya kweli kuhusu shetani, Shetani: (4)**
_____ Yeye ni mwekundu na mwenye pembe na kwato.
_____ Nyumba yake iko kuzimu.
_____ Anapenda watu.
_____ Anaweza kuonekana kama malaika wa mbinguni.
_____ Hawezi kufanya miujiza.
_____ Yeye ni mwongo na muuaji.
_____ Anaweza kuita moto kutoka mbinguni.
_____ Watu wengi watamfuata na kupotea.

**7. Ni mambo gani kati ya haya hapa chini ni ya kweli kuhusu anguko la Adamu na Hawa? (3)**

_____ Shetani alijigeuza kuwa malaika.
______Shetani alimwita Mungu mwongo.
_____ Tunajua Shetani aliwapa tufaha/apple.
_____ Shetani alikuja kwa Adamu kwanza.
______Shetani alitumaini wangekuwa wenye dhambi wasioweza kufa.
_____ Katika kuwajaribu, Shetani alichanganya uongo na Ukweli.

**8. Ni nini Ukweli kuhusu adhabu ya mwisho ya Shetani? (4)**

_____ Atageuka kuwa majivu motoni.
_____ Malaika zake watatoroka.
_____ Moto utakuwa mbinguni.
______Shetani na malaika zake watakubali kuwa walikosea.
_____ Moto pia utaangamiza dhambi na wenye dhambi.
_____ Shetani atakiri haki ya Mungu.

**9. Kwa nini Mungu hakumuua Lusifa alipotenda dhambi? (4)**

_____ Malaika wanaweza kutoelewa.
_____ Wengine wanaweza kuwa na hofu ya Mungu.
_____ Lusifa alikuwa na nguvu sana kwa Mungu.
_____ Malaika wema hawakumruhusu.
_____ Muda ulihitajika ili kuonyesha mpango wa Lusifa.
_____ Muda ulihitajika ili kuthibitisha mpango wa Mungu.

**10. Ni jambo gani moja ambalo hatimaye litatetea serikali ya Mungu? (1)**

_____ Mungu atafanya miujiza fulani.
_____ Kila nafsi katika ulimwengu itapiga magoti, kukiri upendo na haki ya Mungu.
_____ Malaika wa mbinguni watamwomba kila mtu amtumikie Mungu.

**11. Ni mambo gani yaliyo kweli hapa chini kuhusu dhambi? (5)**

_____ Yesu amefanya uharibifu wa dhambi kuwa hakika.
_____ Dhambi ni kuvunja sheria ya Mungu.
_____ Dhambi hututenganisha na Mungu.
_____ Dhambi ni rahisi kuishinda.
______Shetani alivumbua dhambi ya kusema uwongo.
_____ Baada ya kuharibiwa, dhambi haitainuka tena.

**12. Ni vitu gani vilivyo hapa chini ambavyo ni vya kweli? (5)**

_____ Shetani anahusisha/anambambika tabia zake kwa Mungu.
_____ Mungu anatupenda zaidi kuliko wazazi wetu.
_____ Yale anayoitwa “matendo ya Mungu” kama mafuriko au maafa ni matendo ya Shetani.
_____ Maisha ya Yesu yalidhihirisha tabia ya Mungu.
_____ Mungu Baba ni mkali.
_____ Watu wengi hawamwelewi Mungu.

# Uokoaji kutoka Juu au Wokovu kutoka Mbinguni

**Maandiko:** Yeremia 31:3 , 1 Yohana 4:9-10 , Warumi 5:8
**Somo la 3**

Hebu wazia utisho wa kukwama katika bahari na papa wenye njaa na hatari anakaribia! Kisha fikiria jinsi ungefurahi na kufarijiwa kwa kutolewa hadi kwenye salama. Ukweli ni kwamba, kila mtu kwenye sayari hii amepotea katika bahari iliyojaa hatari. Tunahitaji uokoaji haraka, si kutoka kwa mashua au helikopta, lakini kutoka kwa Baba yetu wa Mbinguni. Mungu anakupenda sana hivi kwamba alimtuma Mwanawe kukuokoa. Bila shaka umesikia haya yote hapo awali, lakini una uhakika unaelewa ni nini hasa? Je, Inamaanisha nini kwako, na Je, inaweza kubadilisha maisha yako? Soma na ujue!

Mungu anakujali wewe binafsi. Ni sababu nzuri kama nini ya kushangilia!

### 1. Je, kweli Mungu ananijali?

Hivi ndivyo asemavyo: "Ulikuwa wa thamani machoni Pangu, ulikuwa mwenye kuheshimiwa, Nami nimekupenda." Isaya 43:4 . "Naam, nimekupenda kwa upendo wa milele." Yeremia 31:3 .

**Jibu:** Upendo usio na mwisho wa Mungu kwako na kwangu ni zaidi ya ufahamu wetu. Bwana Anakupenda kana kwamba wewe ndiye nafsi pekee iliyopotea katika ulimwengu. Yeye Angetoa uhai Wake kwa ajili yako au mimi hata kama hapangekuwa na mwenye dhambi mwingine wa kumkomboa. Usijaribu kamwe kusahau Ukweli huu. Wewe ni wa thamani machoni Pake. Anakupenda.

**Kamwe hakujawa na onyesho lingine la upendo kubwa kama msalaba.**

### 2. Mungu ameonyeshaje upendo wake kwetu?

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16 . "Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu alimtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa Yeye. Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba Yeye alitupenda sisi akamtuma Wake. Mwana awe kipatanisho kwa dhambi zetu." 1 Yohana 4:9 , 10 .

**Jibu:** Kwa sababu alitupenda sana, alikuwa tayari kuona Mwanawe wa pekee akiteseka na kufa kuliko kutengwa na wewe na mimi milele. Hatutaweza kuelewa, lakini Yeye alifanya hivyo - kwa ajili yako tu, kwa ajili yangu tu!

**Hakuna mtu ambaye amewahi kuishi ambaye Yesu hakumpenda.**

**3. Angewezaje kumpenda mtu kama mimi?**

“Lakini Mungu aonyesha pendo Lake Yeye Mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.” Warumi 5:8 .

**Jibu:** Hakika si kwa sababu nilichuma au nilistahiki. Hakuna hata mmoja wetu amechuma chochote isipokuwa mshahara wa dhambi, ambao ni mauti ( Warumi 6:23 ). Lakini upendo wa Mungu hauna masharti. Anawapenda wezi, wazinzi na wauaji. Pia anampenda mbinafsi, mnafiki, na yule anayekufuru kwamba hakuna Mungu. Lakini, kubwa kuliko yote, Ananipenda mimi! Na kwa sababu anajua kwamba dhambi zangu zinaweza kusababisha huzuni na kifo tu, Yeye anataka kuniokoa kutoka kwa dhambi zangu. Ndiyo maana alikufa.

**Kifo cha Yesu kilikuwa malipo kamili kwa kila dhambi ambayo ungeweza kuifanya. Unapokubali zawadi hii ya ajabu, unakuwa sehemu ya familia ya kibinafsi ya Yesu.**

**4. Kifo chake kinanifanyia nini?**

“Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu.” 1 Yohana 3:1 . “Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina Lake.” Yohana 1:12 .

**Jibu:** Kristo alikufa ili kutosheleza hukumu ya kifo dhidi yangu. Alizaliwa kama mwanadamu ili apate mateso ya aina ya kifo ninachostahil mimi. Kisha akajitolea kunipa sifa kwa yale aliyoyafanya. Kwa maneno mengine, maisha Yake yasiyo na dhambi yanahesabiwa katika akaunti yangu ili nihesabiwe kuwa mwenye haki. Kifo Chake kinakubaliwa na Mungu kama malipo kamili ya makosa yangu yote ya zamani, na kwa mimi kukubali kile alichofanya msalabani kama zawadi, ninachukuliwa katika familia ya Mungu kama mtoto Wake. Hii inashanga akili yangu! Tafakari mambo haya rahisi kwa muda:

- Kwa sababu ya dhambi zangu, nimehukumiwa kifo.

- Siwezi kulipa adhabu hiyo bila kupoteza uzima wa milele, kwa sababu ikiwa nilikufa kwa ajili ya dhambi zangu, singeweza kujifufua mwenyewe. Ningekuwa nimekufa milele.

- Nina deni ambalo siwezi kulilipa! Lakini rafiki anakuja, katika utu wa Yesu, na kusema, “Nitalipa. Nitakufa badala yako na kulipa deni kwa ajili yake. Hautalazimika kufa kwa ajili ya dhambi zako.”

- Lazima nikubali ofa nzuri hii! Je, jambo hili si rahisi? Ninakiri waziwazi na kukubali kifo Chake kwa ajili ya dhambi zangu. Wakati ninapofanya hivi, nimekuwa mwana au binti wa Mungu!

**Yesu alitoa maisha Yake ili kulipa deni usiloweza kulipa.**

**5. Je, mimi ninampokeaje na hivyo kutoka mautini kuingia uzimani?**

**Kubali mambo matatu tu:**

**1.** Mimi ni mwenye dhambi. “Wote wamefanya dhambi.” Warumi 3:23 .
**2.** Nimehukumiwa kufa. “Mshahara wa dhambi ni mauti.” Warumi 6:23 .
**3.** Siwezi kujiokoa. “Bila mimi hamwezi kufanya lolote.” Yohana 15:5 .

**Kisha, amini mambo matatu:**

**1. Yeye** Alikufa kwa ajili yangu. “Kwamba ... anapaswa kuonja mauti kwa ajili ya kila mtu.” Waebrania 2:9.

**2. Yeye** Ananisamehe. “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu.” 1 Yohana 1:9.

**3. Yeye** Ananiokoa. “Yeye aniaminiye yuna uzima wa milele.” Yohana 6:47 .

**Jibu:** Kwa kuomba, kuamini, na kukubali zawadi kuu ya Mungu, Bwana wetu Yesu Kristo.

**Je, unazama katika dhambi? Yesu atakuokoa mara moja ikiwa utamwomba.**

**6. Je, ni lazima nifanye nini ili kupata zawadi hii ya wokovu?**

“Wanahesabiwa haki bure kwa neema Yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu.” Warumi 3:24 . “Mtu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria.” Warumi 3:28 .

**Jibu:** Kitu pekee ninachoweza kufanya ni kuikubali kama zawadi safi. Kazi zangu za utii hazitanisaidia hata kidogo katika uzoefu wa kuhesabiwa haki. Wote wanaoomba wokovu kwa imani wataupokea. Mtenda dhambi mbaya zaidi atakubaliwa kwa msingi ule ule kama mtenda-maadili zaidi. Yaliyopita hayahesabiki. Kumbuka, Mwenyezi Mungu anawapenda wote sawa, na msamaha ni wa wale wanauomba. “Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.” Waefeso 2:8 , 9 .

**Nguvu za Yesu humbadilisha mwenye dhambi na mwenye kuchukiza kuwa mtakatifu mwenye upendo.**

**7. Ninapojiunga na familia Yake Mungu kwa njia ya imani, Yesu anafanya mabadiliko gani katika maisha yangu?**

“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya.” 2 Wakorintho 5:17 .

**Jibu:** Kristo anapopokelewa moyoni mwangu, Yeye Anaharibu utu wa zamani wa dhambi na kwa kweli Yeye Ndiye hunibadilisha kuwa kiumbe kipya cha kiroho.

Maisha ya zamani ya dhambi sasa yanakuwa ya kuchukiza na yasiyofaa. Kwa furaha naanza kupata uzoefu, kwa mara ya kwanza, uhuru mtukufu kutoka kwa hatia na hukumu. Ninaanza kuona jinsi maisha ambavyo yangu yamekuwa matupu bila Kristo. Badala ya kula maganda ya ndizi/matunda chini ya meza, sasa ninakula karamu ya Mfalme. Kwa Dakika moja tu, Mungu hutoa furaha zaidi kuliko maisha ya kumtumikia shetani. Ni mabadilishano ya ajabu kama nini! Kwa nini nilisubiri kwa muda mrefu kukubali zawadi hii?

**Zawadi yenye thamani zaidi ambayo wazazi wanaweza kuwapa watoto wao ni** kuwa Wakristo.

**8. Je, maisha haya yaliyobadilika yatakuwa kweli ya furaha kuliko starehe za maisha ya zamani?**

Yesu alisema: "Hayo nimewaambia ... ili furaha yenu iwe kamili." Yohana 15:11 . "Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli." Yohana 8:36 . "Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele." Yohana 10:10 .

**Jibu:** Wengi wanahisi kwamba maisha ya Kikristo hayatakuwa ya furaha kwa sababu ya vizuizi na kujinyima. Kinyume kabisa ndiyo Kweli. Unapokubali upendo wa Yesu, furaha ya ajabu huchipuka kutoka ndani. Amani na furaha isiyo na kifani hutawala maishani mwako. Hapa tunaongea juu ya msisimko wa furaha! Hakuna cha kulinganisha na maisha ya zamani ya ubinafsi na kushindwa/kufeli. Kama ndoto mbaya, wakati uliopita wenye uchungu hufifia, na unapata maisha "kwa wingi zaidi, yaani tele," jinsi Mungu alivyokusudia iwe.

**Yesu anapoingia katika maisha yako, nguvu Zake za miujiza hubadilisha utiifu kutoka mzigo hadi furaha kuu.**

**9. Lakini je, ninaweza kujifanya nifanye mambo yote ambayo Mkristo anapaswa kufanya?**

Nimesulubiwa pamoja na Kristo; wala si mimi, bali Kristo yu hai ndani yangu." Wagalatia 2:20. "Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu." Wafilipi 4:13 .

**Jibu:** Hapa ndipo muujiza mkuu wa maisha ya Kikristo unapofunuliwa. Hakuna kujilazimisha kuwa mzuri! Unachofanya kama Mkristo ni kutokeza kwa maisha ya Mtu mwingine ndani yako (maisha ya Yesu). Utii ni mwitikio wa asili wa upendo katika maisha yako. Kuzaliwa na Mungu, kama kiumbe kipya, unataka kumtii kwa sababu maisha Yake yamekuwa sehemu ya maisha yako. Kumpendeza mtu unayempenda sio mzigo, lakini ni furaha. "Kuyafanya mapenzi Yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; naam, sheria Yako imo moyoni mwangu." Zaburi 40:8

**Si vigumu kumpendeza mtu unayempenda kwa dhati.**

**10. Je, unamaanisha kwamba hata zile Amri Kumi hazingekuwa ngumu kuzitii?**

“Mkinipenda, mtazishika amri Zangu.” Yohana 14:15 . “Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri Zake; wala amri Zake si nzito.” 1 Yohana 5:3 . “Lakini yeye alishikaye Neno Lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli.” 1 Yohana 2:5 .

**Jibu:** Biblia daima hufungamanisha utiifu kwa uhusiano wa upendo. Wakristo waliozaliwa mara ya pili hawaoni kuwa ni kazi ya kuchosha kuzishika Amri Kumi. Huku dhambi zote zilizopita zikiwa zimefunikwa na kifo Chake cha upatanisho, utiifu wangu wa sasa na ujao unatokana na maisha Yake ya ushindi ndani yangu. Kwa kweli, kwa sababu ninampenda sana kwa kubadilisha maisha yangu, ninaenda zaidi ya matakwa au mahitaji ya Amri Kumi. Kila siku mimi huchunguza Biblia ili kupata dalili za mapenzi Yake, nikijaribu kutafuta njia ndogo zaidi za kuonyesha upendo wangu Kwake. “Na lo lote tuombalo, twalipokea Kwake, kwa kuwa twazishika amri Zake, na *kuyatenda yapendezayo machoni Pake.* ” 1 Yohana 3:22 , mkazo umeongezwa.

**Kushika Amri Kumi katika jaribio la kupata wokovu kutasababisha huzuni na kukata tamaa tu. Lakini mtu ambaye amepitia zawadi ya wokovu anafurahia kutembea katika njia ya utii kwa sheria za Mungu.**

**11. Ninawezaje kuwa na hakika kwamba kushika amri kunakotajwa katika Biblia kwa watu wa Mungu si kushika sheria?**

“Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu.” Ufunuo 14:12 . “Nao [watakatifu] wakamshinda [Shetani] kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.” Ufunuo 12:11 .

**Jibu:** Usichanganye utii na ushupavu wa sheria (uhalali, legalism), ushupavu wa sheria ni kujaribu kupata wokovu kwa matendo mema. Watakatifu wanatajwa katika Biblia kuwa na sifa nne: (1) Wanashika amri, (2) Wanaamini damu ya Mwana-Kondoo, (3) Wanashiriki imani yao na wengine, na (4) Wanachagua kufa badala ya kutenda dhambi. Hizi ndizo alama za Kweli za mtu ambaye yuko katika upendo na Kristo na ambaye amejitolea maishani kumfuata.

**Ubatizo ni sherehe ya ndoa ambayo inanileta kwa Kristo.**

**12. Ni tendo gani la maana linalotia muhuri uhusiano wa upendo pamoja na Kristo, nalo linaashiria nini?**

“Basi tulizikwa pamoja Naye kwa njia ya ubatizo katika mauti Yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.” “Ili mwili wa dhambi uharibiwe.” Waroma 6:4, 6 . “Naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi.” 2 Wakorintho 11:2 .

**Jibu:**

Ubatizo unaashiria matukio matatu muhimu katika maisha ya mwamini wa kweli: (1) kifo kwa dhambi, (2) kuzaliwa kwa maisha mapya katika Kristo, na (3) ndoa na Kristo kwa umilele. Muungano huu wa kiroho utazidi kuwa na nguvu na uzuri/utamu kadiri wakati unavyoendelea, maadamu upendo unaendelea kukua. Kama ilivyo katika ndoa yoyote, kupotea kwa upendo kunaweza kugeuza paradiso kuwa jehanamu. Upendo unapotoweka, nyumba inashikiliwa pamoja na wajibu wa kufanya vitu kama mashine tu au alimradi, kwa vile kuna kulazimishwa kwa sheria ya ndoa. Vivyo hivyo, Mkristo anapoacha kumpenda Kristo kwa moyo wake wote, dini yake inakuwepo tu kama utiifu wenye vizuizi kwa lundo au seti ya kanuni.

**Upendo wangu kwa Yesu unaongezeka ninaposhiriki na wengine.**

**13. Ninawezaje kuwa na hakika kwamba imani na upendo wa ndoa yangu kwa Kristo utaendelea kuongezeka?**

"Tafuta maandiko." Yohana 5:39 . "Ombeni bila kukoma." 1 Wathesalonike 5:17 . "Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye." Wakolosai 2:6 . "Mimi hufa kila siku." 1 Wakorintho 15:31 .

**Jibu:** Hakuna mapenzi yanaweza kufanikiwa bila mawasiliano. Maombi na kujifunza Biblia ni muhimu kabisa ili kudumisha uhusiano huu kukua. Neno Lake linajumuisha barua ya upendo ambayo ni lazima niisome kila siku ili kulisha maisha ya kiroho. Kuzungumza Naye katika sala huimarisha kujitoa na hufungua akili yangu kwa ujuzi wa kusisimua na wa kindani zaidi wa kujali Kwake kwangu. Kila siku nashangaa kugundua habari za majaliwa Yake ya ajabu kuhusu furaha yangu.

**Mungu Anafunga Ndoa Yetu ya Kiroho**

Ili kutia muhuri ndoa yetu ya kiroho kwa umilele, Yeye ameahidi hataniacha kamwe ( Zaburi 55:22 ) Mathayo 28:20 Waebrania 13:5 ), kunitunza katika ugonjwa au katika afya ( Zaburi 41:3 ) Isaya 41:10 ), na kuniandalia kila hitaji ambalo lingeweza kutokea katika maisha yangu ( Mathayo 6:25-34 ). Kama vile nilivyompokea kwa imani na kupata ahadi Zake kuwa za kutosha, basi mimi ninaendelea kumtumaini kwa kila hitaji la wakati ujao, na Yeye haniachi kamwe.

**14. Ni shauku yangu kumwalika Yesu katika maisha yangu na kupata uzoefu wa kuzaliwa upya.**

**Jibu:**

# MASWALI YA KUPEKECHA KICHWA

**1. Je, kifo cha Mtu mmoja kingewezaje kulipa adhabu ya dhambi za wanadamu wote? Nimeishi maisha ya kutisha ya dhambi. Ninaogopa kwamba Mungu angefanya jambo la pekee sana ili kumfidia mtu mbaya sana kama mimi.** Warumi 3:23 inatuambia kwamba "wote wamefanya dhambi." Kwa sababu "mshahara wa dhambi ni mauti" ( Warumi 6:23 ) na kwa kuwa "wote wamefanya dhambi," kwa hiyo "msaada wa pekee" unahitajika kwa kila mtu ambaye amezaliwa. Mmoja tu Ndiye ambaye maisha Yake yako sawa, yaani kamili katika wanadamu wote, Naye angeweza kufa kwa ajili ya dhambi za jamii ya ubinadamu. Kwa sababu Yesu Ndiye Muumba na Mwanzilishi wa uhai wote, maisha aliyotoa yalikuwa sawa na maisha ya watu wote ambao wangeishi milele. Sio tu kwamba upatanisho ulipaswa kufanywa na Yule ambaye uhai Wake ungeweza kusimama kwa ajili ya viumbe vingine vyote vilivyoumbwa, lakini Yule aliyekufa kifo cha upatanisho alipaswa kuwa na uwezo wa kufufuka kutoka katika kifo hicho. Kwa nini? Ili kusimamia faida za upatanisho kwa wote ambao wangeuomba kwa imani. "Kwa hiyo Yeye aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa Yeye; maana Yu hai sikuzote ili kuwaombea." Waebrania 7:25 .

**2. Nikimkubali Kristo na msamaha Wake na kisha kuanguka tena, Je, atanisamehe tena?**

Tunaweza kumwamini Mungu kutusamehe tena ikiwa tutajutia dhambi zetu na kuziungama. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yohana 1:9 .

**3. Ninawezaje kumwendea Mungu katika hali yangu ya dhambi? Je! haingekuwa bora kwangu kuwa na mchungaji, kasisi au mhudumu aniombee?**

Kwa kuwa Yesu Kristo aliishi katika mwili na "alijaribiwa kama sisi" ( Waebrania 4:15 ), tuna Mungu anayeweza kuelewa na ambaye anatamani kuwa na rehema kwetu. Waebrania 4:16 inatuambia tunaweza "kukikaribia kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema." Tunaweza kumwendea Mungu moja kwa moja kupitia Yesu Kristo, bila mpatanishi; na kutumaini rehema Zake, tunaweza "kwa ujasiri" kuja Kwake katika Jina la Yesu ( Yohana 14:14 ). 1 Timotheo 2:5 inasomeka hivi: "Kwa maana kuna Mungu mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu.

**4. Je, kuna jambo lolote ninaloweza kufanya ili kumsaidia Mungu kuniokoa?** Hapana. Mpango Wake ni wa neema kabisa ( Warumi 3:24 ; 4:5 ); ni "zawadi ya Mungu." Waefeso 2:8 . Ni kweli kwamba Mungu anapotujalia neema kupitia imani, anatupa pia hamu na nguvu ya kumtii. Hii inasababisha kufuata sheria Zake. Kwa hiyo, hata utii huu unatokana na neema ya bure ya Mungu. Utiifu—huduma na utii wa upendo—ndio jaribu la Kweli la ufuasi na tunda la asili la imani katika Yesu Kristo.

**5. Ikiwa Mungu atanisamehe dhambi Zangu na kunirudisha katika familia Yake, je, hilo litaondoa adhabu yoyote ya wakati ujao kwa ajili ya dhambi zangu, au bado nitahitajika kufanya aina fulani ya toba?** Maandiko yanasema, "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu." Warumi 8:1 . Kristo alilipa adhabu kamili kwa ajili ya makosa yetu, na wale wanaomkubali kwa imani hawana deni la matendo ya toba ya kutakaswa, lakini tayari wanachukuliwa kuwa "wameoshwa" katika damu ya Mwana-Kondoo! Isaya 43:25 ina ahadi nzuri ya msamaha: "Mimi, naam, Mimi, Ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili Yangu Mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako." Mika 7:18 , 19 huonyesha mtazamo mzuri wa Mkombozi-Mungu kuelekea watu Wake: "Ni nani aliye Mungu kama Wewe, Mwenye kusamehe uovu, na kulipita kosa la mabaki ya urithi Wake? milele, kwa kuwa wapendezwa na rehema. Atageuka tena, atatuhurumia, atayatiisha maovu yetu; Nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari."

## MASWALI YA CHEMSHA BONGO KWIZZ

**1. Mungu alimwaga mbingu yote katika zawadi gani kuu kwa mwanadamu? (1)**
_____ Biblia.
_____ Kanisa lake.
_____ Yesu Kristo.
_____ Sheria.

**2. Onyesho kuu la upendo ambalo ulimwengu umewahi kuona lilikuwa (1)**
_____ Mikate na samaki.
_____ Kifo cha Yesu msalabani.
_____ Pentekoste.
_____ maungamo ya Petro.

**3. Dhabihu ya Kristo msalabani ilikuwa kwa ajili ya (1)**
_____ Kila mtu.
_____ Wenye haki pekee.
_____ Waovu tu.
_____ Wale waliochaguliwa tangu awali kwa ajili ya wokovu.

**4. Mungu anampenda zaidi mtu wa aina gani? (1)**
_____ Washiriki wa Kanisa.
_____ Makahaba na wezi.
_____ Kila mtu sawa.
_____ Wakristo waliozaliwa mara ya pili.

**5. Kristo alizaliwa katika familia ya wanadamu ili (1)**
_____ Alipe adhabu ya dhambi.
_______ Ajue jinsi tulivyo dhaifu.
_____ Awe seremala mzuri.

**6. Ili kupata wokovu, mtu lazima (1)**
_____ Asome kozi ya Biblia.
_____ Awe mshiriki wa kanisa.
_____ Anene kwa lugha.
_____ Aipokee kama zawadi.

**7. Tunaokolewa kwa (1)**
_____ Matendo mema.
_____ Neema.
_____ matamanio.

**8. Msamaha na kukubalika hutuongoza kuhisi (2)**
_____ Kwamba tunaweza kuanza kutenda dhambi tena.
_____ Majuto ya raha zilizokataliwa.
_____ Furaha na amani.
_____ Uhakikisho wa uzima wa milele.

**9. Utii unapaswa kutegemea (1)**
_____ Hofu ya kuzimu.
_____ Hamu ya kupata idhini ya marafiki.
_____ Upendo kwa Yesu.

**10. Mwenendo wa Kikristo, au kushika amri, ni (1)**
_____ Kuwa mshika sheria (legalist).
_____ Moja ya matunda ya uongofu wa kweli.
_____ Sio muhimu.

**11. Ndoa kwa Kristo inafananishwa na (1)**
_____ Kujiunga na utawa au monasteri.
_____ Ubatizo.
_____ Pete ya harusi inavyovaliwa mkono wa kulia.
_____ Kuweka nadhiri ya useja.

**12. Njia kuu mbili za kukaa katika upendo na Kristo ni (2)**
_____ Kusoma Biblia kila siku.
_____ Kutoa sadaka ya ukarimu.
_____ Kujiepusha na nyama ya nguruwe.
_____ Mtazamo wa kudumu wa maombi.

# Jiji la Angani la kushangaza (Collosal City)

**Somo la 4**
Ongea juu ya jiji kubwa! Hebu wazia mji au jiji lako unalolipenda bila mashimo yoyote barabarani, foleni ya magari, uchafuzi wa mazingira, au uhalifu wa aina yoyote! Unasema haiwezekani? Biblia inatuambia kuhusu jiji lenye barabara zilizojengwa kwa dhahabu! Na ndani ya kuta zake ndefu zilizotengenezwa kwa yaspi safi, hakutakuwa na hata mtu mmoja anayekohoa, anayepiga chafya, au kupatwa na mafua. Kila mtu atakuwa na afya kamilifu na atafurahia ushirika wa kila mmoja. Je, ungependa kutembelea jiji hili? Kweli, sio tu kwamba unaweza kutembelea hilo jiji , bali pia unaweza kuishi humo! Soma ili kujua jinsi…New York, Tokyo, na London si kitu kwa kulinganisha! Subiri tu hadi uelewe Ukweli wa kushangaza kuhusu jiji hili kubwa ambalo linaweza kusafiri angani. Yote ni Ukweli, sio hekaya za kisayansi! Maelezo katika Mwongozo huu wa Somo yatafurahisha nafsi yako na kukupa tumaini la siku zijazo.

Mungu Ndiye mbunifu na mjenzi wa mji mtakatifu.

**1. Ni nani mbunifu na mjenzi wa jiji hili la anga?**

"Kwa hiyo Mungu haoni aibu kuitwa Mungu wao; maana amewaandalia mji." Waebrania 11:16 .
**Jibu:** Biblia inatangaza kwamba Mungu anajenga mji mkuu kwa ajili ya watu Wake. Na mji huu ni halisi na halisi kama yoyote ambayo umewahi kuijua au kuishi.

Mji wa ajabu wa Mungu uko mbinguni, makao Yake Bwana.

**2. Uko wapi mji huu wa ajabu ambao Mungu anatayarisha?**
"Nami mimi Yohana nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu mbinguni." Ufunuo 21:2 . "Ee Bwana, Mungu wangu ... usikie huko mbinguni, makao yako." 1 Wafalme 8:28-30 .
**Jibu:** Mji huu mkubwa unaojengwa, kwa sasa, uko katika anga ya mbali sana katika makao ya Mungu, yaitwayo mbinguni.

Angalia ukubwa wa jiji ukilinganishwa na majimbo kadhaa.

3. Maandiko yanaelezaje kuhu jiji hili la ajabu la angani?

**Jibu:**

**(A) UKUBWA**
"Mji ule una mraba, na urefu wake ulikuwa kama upana wake; akaupima mji kwa ule mwanzi, umbali wa maili kumi na mbili elfu." Ufunuo 21:16 . Mji ni mraba kabisa. Mzingo wake takribani 2400 km, au maili 1,500 (furlong ni 1/8 maili). Una urefu wa maili 375 kila upande au takribani ya km 600.

### (B) JINA
Mji unaitwa “Yerusalemu mpya” katika Ufunuo 21:2 .

### (C) KUTA
“Akaupima ukuta wake, dhiraa mia na arobaini na nne… Na jengo la ukuta wake lilikuwa la yaspi.” Ufunuo 21:17 , 18 . Ukuta wa dhiraa 144, au urefu wa futi 216 (dhiraa moja ni inchi 18), unazunguka jiji hilo. Ukuta umejengwa kwa yaspi imara, yenye mng’ao na uzuri usio na maelezo. Fikiria jambo hilo! Karibu orofa 20 za madini ya yaspi thabiti!

### (D) MILANGO
“Na ilikuwa na milango kumi na miwili ….. Upande wa mashariki milango mitatu upande wa kaskazini milango mitatu upande wa kusini milango mitatu na magharibi milango mitatu.” Na ile milango kumi na miwili ilikuwa lulu kumi na mbili, kila lango moja lilikuwa la lulu moja.” Ufunuo 21:12 , 13 , 21 . Mji huo una milango 12 - mitatu kila upande - kila moja umetengenezwa kwa lulu moja.

### (E) MISINGI
“ Ukuta wa mji ulikuwa na misingi kumi na miwili … iliyopambwa kwa kila aina ya mawe ya thamani.Msingi wa kwanza ulikuwa yaspi; wa pili yakuti samawi; wa tatu kalkedoni; wa nne zumaridi;

[20] wa tano sardoniki; wa sita akiki; wa saba krisolitho; wa nane zabarajadi; wa kenda yakuti ya manjano; wa kumi krisopraso; wa kumi na moja hiakintho; wa kumi na mbili amethisto.” Ufunuo 21:14-20 . Jiji lina misingi 12 kamili, iliyokamilika kila moja iliyojengwa kwa mawe ya thamani. Kila rangi ya upinde wa mvua itawakilishwa, kwa hiyo kwambali jiji hilo bila shaka litaonekana kuwa likitulia/likikaa juu ya upinde wa mvua

### (F) MITAA
“Barabara ya mji ilikuwa dhahabu safi, kama kioo angavu.” Ufunuo 21:21

### G) INAVYOONEKANA
“Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.” “Akiwa na utukufu wa Mungu; na nuru yake ilikuwa kama jiwe la thamani kuu, kama jiwe la yaspi, angavu kama bilauri.” “Urefu na upana na kimo chake ni sawa [sawa].” Ufunuo 21:2 , 11 , 16 .Mji huo, pamoja na vito vyake vyote vya thamani, dhahabu, na uzuri unaometa-meta, utaangazwa kwa utukufu wa Mungu. Katika utukufu wake wa kuvutia na usafi inalinganishwa na “bibi arusi aliyepambwa kwa mumewe.”

Mti wa ajabu wa uzima wa mbinguni huleta uzima na ujana usio na mwisho kwa wote wanaoula.

**4. Ni jambo gani la ajabu la jiji hili tukufu linalomhakikishia kila raia nguvu na ujana wa milele?**
“Katikati ya njia kuu yake, na upande huu wa ule mto, palikuwa na mti wa uzima, uzaao matunda ya namna kumi na mbili, wenye kuzaa matunda yake kila mwezi;

na majani ya mti huo yalikuwa ya uponyaji. mataifa.” Ufunuo 22:2 . “Chukua matunda ya mti wa uzima, ule, na uishi milele.” Mwanzo 3:22 .

**Jibu:** Mti wa uzima, unaozaa aina 12 za matunda (na uko katikati ya jiji-- Ufunuo 2:7 ), huleta uzima na ujana usio na mwisho kwa wote wanaoshiriki. Hata majani yake yatakuwa na sifa nzuri za kudumu. Mti huu utatoa mazao mapya ya matunda kila mwezi.
Mji mtakatifu utashuka duniani na kuwa mji wake mkuu.

**5. Je, ni kweli kwamba jiji hili la ajabu litashuka duniani?**
“Nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu mbinguni, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Ufunuo 21:2 . “Heri wenye upole; maana hao watairithi nchi.” Mathayo 5:5 . “Wenye haki watalipwa duniani.” Mithali 11:31 .

**Jibu:** Ndiyo, jiji hilo takatifu la fahari litashuka kwenye dunia hii na kuwa jiji kuu la dunia iliyofanywa upya. Wenye haki wote watakuwa na makao katika mji huu.

Dhambi na wenye dhambi wataangamizwa kwa moto kutoka kwa Mungu.

**6. Nini kitatokea kwa dhambi na wenye dhambi?**
“Wote wenye kiburi, naam, na wote watendao uovu watakuwa makapi; na siku inayokuja itawateketeza.” Malaki 4:1 . “Moto ulishuka kutoka kwa Mungu kutoka mbinguni, ukawala.” Ufunuo 20:9 . “Viumbe vya asili vitayeyuka kwa joto kali, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketezwa.” 2 Petro 3:10 . “Mtawakanyaga waovu; kwa maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu.” Malaki 4:3 . “Lakini kama ilivyo ahadi yake, tunatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake.” 2 Petro 3:13 .

**Jibu:** Mungu ataangamiza dhambi na wenye dhambi wote kwa moto. Moto huu utayeyusha dunia na kugeuza kila kitu kuwa majivu. Kisha Mungu atafanya dunia mpya kamilifu, na jiji takatifu litakuwa makao yake makuu. Hapa wenye haki wataishi kwa furaha, amani, na utakatifu milele. Mungu anaahidi kwamba dhambi haitainuka tena. Angalia Nahumu 1:9 .

Katika ufalme Wake mpya Bwana ataishi kibinafsi kati ya watu Wake.

**7. Ni ahadi gani zenye kuburudisha na zenye kusisimua ambazo Mungu huwatolea watu wanaoingia katika ufalme Wake mpya?**

**Jibu:**
A. Bwana, ana kwa ana, ataishi pamoja nao ( Ufunuo 21:3 ).

B. Hawatawahi kuchoka. Kutakuwa na furaha milele na milele ( Zaburi 16:11 ).

C. Hakutakuwa tena na kifo, maumivu, machozi, huzuni, magonjwa, hospitali, upasuaji, misiba, kukata tamaa, shida, njaa, kuachana, kupigwa au kiu ( Ufunuo

21: 4 ) Isaya 33:24 Ufunuo 22:3 Isaya 65:23 Ufunuo 7:16 ).

D. Hawatachoka ( Isaya 40:31 ).

E. Kila mtu aliyeokoka atakuwa mzima kimwili kwa kila njia. Viziwi watasikia, vipofu wataona, mabubu wataimba, na viwete wataweza kukimbia ( Isaya 35:5 , 6) Wafilipi 3:21 ).

F. Wivu, woga, chuki, uwongo, husuda, uchafu, wasiwasi, uchafu, wasiwasi, na uovu wote vitafungiwa nje ya ufalme wa Mungu milele ( Ufunuo 21:8 , 27 ) 22:15 ). Watu hawatalemewa tena na mahangaiko na masumbufu yanayowasukuma kukengeushwa. Hakutakuwa na kuvunjika kwa mishipa ya fahamu tena kwaajili ya wasiwasi. Wakati utakuwa ni wa umilele tu, na misongo na tarehe ya mwisho ya kuwasilisha jambo na presha yake vitaisha milele (no deadlines).

Bahari kubwa za leo hazitakuwepo katika ufalme mpya wa Mungu.

**8. Dunia mpya itakuwa tofauti jinsi gani na dunia yetu leo?**
**Jibu:**
A. Bahari kuu kama tunavyozijua leo zitatoweka (Ufunuo 21:1). Bahari kubwa na ndogo za maji ya chumvi hufunika robo tatu ya uso wa dunia leo. Hii haitakuwa hivyo katika ufalme mpya wa Mungu. Ulimwengu wote utakuwa bustani moja kubwa ya uzuri usio na kifani, iliyoingiliana na maziwa, mito, na milima (Ufunuo 22:1). Matendo 3:20, 21).

B. Majangwa yatakuwa bustani ( Isaya 35:1 , 2 ).

C. Wanyama wote watakuwa wapole kama wale wa kufugwa ( na pengine bora zaidi maana hata wanyama wa kufungwa wanaweza kuwa hatari). Hakuna atakayemwinda mwingine, na mtoto mdogo atawaongoza ( Isaya 11:6-9). 65:25 ).

D. Hakutakuwa na laana tena ( Ufunuo 22:3 ).

E. Hakutakuwa na jeuri ya aina yoyote tena ( Isaya 60:18 ). Mbingu inaondoa kabisa uhalifu, dhoruba, mafuriko, matetemeko ya ardhi, vimbunga, majeraha, nk.

F. Hakuna chochote kichafu kitakachopatikana katika dunia mpya ( Ufunuo 21:27 ). Hakutakuwa na vipande vya sigara, mate ya ugoro, walevi, vilabu vya pombe, vinywaji vyenye kileo, madanguro, picha chafu, au uovu mwingine wowote au uchafu wa aina yoyote.

Watoto, watacheza pamoja, nao watajaza mitaa ya Yerusalemu mpya.

**9. Je, kutakuwa na watoto katika ufalme wa Mungu? Ikiwa ndivyo, watakua?**
"Na mitaa ya mji itajaa wavulana na wasichana, wakicheza katika njia zake." Zekaria 8:5 . "Nanyi mtatoka nje, na kukua kama ndama wa zizini." Malaki 4:2 .
**Jibu:** Ndiyo, kutakuwa na wavulana na wasichana wengi katika mji mtakatifu (Isaya 11: 6-9 ), na vijana hawa watakua ( Malaki 4: 2 ). Tumepungua sana katika

kimo, akili, na uhai tangu Adamu, lakini yote haya yatarejeshwa (Matendo 3:20 , 21 ).

**10. Je, watu waliookoka watajuana wanapokutana tena na wapendwa wao mbinguni?**
Ndipo nitakapojua kama nijulikanavyo mimi." 1 Wakorintho 13:12 .

**Jibu:** Biblia inafundisha wazi kwamba wapendwa wao waadilifu ambao wamekufa watafufuliwa ili kujiunga na waadilifu wanaoishi katika ufalme wa Mungu (Isaya 26:19 ; Yeremia 31:15-17 ; 1 Wakorintho 15:51-55 ; 1 Wathesalonike 4:13 ) -18). Na Maandiko pia yanafundisha kwamba watu katika ufalme mpya wa Mungu watajuana, kama vile watu wanavyotambuana duniani leo.
Mbinguni watu halisi watapata furaha ya Kweli. Matumaini na matamanio mazuri zaidi ya moyo wa mwanadamu yatatimizwa.

**11. Je, watu mbinguni watakuwa halisi, wenye nyama na mifupa?**
"Yesu Mwenyewe akasimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu.' Wakashikwa na hofu, wakaogopa, wakidhani wameona pepo. Akawaambia, Mbona mnafadhaika? mawazo yatokayo mioyoni mwenu? Tazameni mikono Yangu na miguu Yangu, ya kuwa ni Mimi Mwenyewe; nishikeni, mwone; "Na walipokuwa bado hawajasadiki kwa furaha, wakistaajabu, akawaambia, Mna chakula cho chote hapa? Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa, na sega la asali. Akakitwaa, akala mbele yao. ." "Akawaongoza nje mpaka Bethania, na ... alipokuwa akiwabariki, akajitenga nao, akachukuliwa juu mbinguni." Luka 24:36-39 , 41-43 , 50 , 51 . "Yesu huyu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni." Matendo 1:11 . "Bwana Yesu Kristo ... ataubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu." Wafilipi 3:20 , 21 .

**Jibu:** Baada ya kufufuka Kwake, Yesu aliwathibitishia wanafunzi Wake kwamba Yeye alikuwa nyama na mifupa kwa kuwafanya wamhisi na kwa kula chakula. Yesu huyu huyu wa nyama na mifupa alipaa kwa Baba Yake na atakuja tena duniani. Wenye haki watapewa miili kama mwili wa Kristo na watakuwa watu halisi wenye nyama na mifupa milele. Tofauti itakuwa kwamba mwili wa mbinguni hautakufa, hautaoza, au kuharibika. Fundisho la kwamba wale waliookolewa mbinguni watakuwa ni mizimu inayoelea juu ya mawingu ya ukungu na kutofanya lolote isipokuwa kucheza vinubi halina msingi katika Maandiko. Yesu hakufa msalabani ili kutoa wakati ujao usio na maana ya kipumbavu kwa wale wanaokubali upendo Wake na kufuata njia Yake ya maisha kwa bora na ya uungwana. Watu wengi hawapendezwi na maisha kama haya na, kwa hivyo, wana hamu ndogo ya kuingia huko au hawana kabisa ya matamanio ya kuingia katika ufalme wa mbinguni wa Mungu - mara nyingi wanapendelea kwenda mbinguni tu kwa sababu wanaogopa jehanamu. Laiti watu wote kila mahali wangeweza kujifunza Ukweli kuhusu jiji takatifu la Mungu na dunia mpya, mamilioni wangeanza kuelewa upendo Wake na wangemgeukia kwa mioyo yao yote. Mtu anayekosa ufalme wa Mungu amefanya kosa kuu maishani mwake.

Hakuna lugha ya mwanadamu inayoweza kueleza utukufu na furaha ya muziki safi wa mbinguni.

**12. Wenye haki watatumiaje wakati wao katika ufalme wa mbinguni?**
"Watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu, na kula matunda yake. Hawatajenga, wala hawatapanda mtu kukaa ndani yake, na mwingine atakula; ... mikono yao." Isaya 65:21 , 22 .

**Jibu:** Wenye haki watajenga nyumba zao wenyewe katika ardhi mpya. (Kila mmoja pia atakuwa na jumba la jiji lililojengwa na Kristo-- Yohana 14:1-3 .) Hii yaonyesha watakuwa na nyumba mashambani na mjini! Watapanda mizabibu na kula matunda yake. Biblia iko wazi kabisa. Watu halisi hufanya mambo halisi mbinguni, na watafurahia yote kikamili. Na tutatambuana huko, uso kwa uso hakika, na si roho kwa roho!

Mbingu itatuletea fursa ya kuwa marafiki na wazee wa imani kama Ibrahimu na manabii wa Biblia kama Yohana mbatizaji.

**13. Ni mambo gani mengine yenye kusisimua ambayo waliokombolewa watashiriki?**

**Jibu:** A. Wataimba na kucheza muziki wa mbinguni ( Isaya 35:10 51:11 Zaburi 87:7 Ufunuo 14:2 , 3 ).

B. Wataabudu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu kila Sabato ( Isaya 66:22 , 23 ).

C. Watafurahia maua na miti isiyofifia ( Ezekieli 47:12 Isaya 35:1 , 2 ).

D. Watatembelea wapendwa, wazee wa imani, manabii, n.k. ( Mathayo 8:11 Ufunuo 7:9-17 ).

E. Watajifunza wanyama wa mbinguni ( Isaya 11:6-9 65:25 ).

F. Watasafiri na kuchunguza bila kuchoka ( Isaya 40:31 ).

G.Watamsikiliza Mungu akiimba ( Sefania 3:17 ).

H. Watatambua matamanio mazuri zaidi ( Zaburi 37:3 , 4 Isaya 65:24 ).

I. Furaha kuu zaidi ni ya majaliwa yote ya kuwa kama Yesu, kusafiri pamoja Naye, na kumuona uso kwa uso

( Ufunuo 14:4 ) 22:4 21:3 1 Yohana 3:2 ).

Mbingu zitakuwa zenye utukufu na thawabu zaidi kuliko chochote tunachoweza kuwazia.

**14. Je, lugha dhaifu ya kibinadamu inaweza kuelezea Kweli utukufu wa makao ya mbinguni?**
"Mambo ambayo jicho halijaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. 1 Wakorintho 2:9 .
**Jibu:** Hata katika ndoto zake za kustaajabisha zaidi, moyo wa mwanadamu hauwezi kuanza kufahamu maajabu ya ufalme wa milele wa Mungu. Yote ambayo Adamu alipoteza yatarejeshwa ( Matendo 3:20 , 21 ).

Yesu anatayarisha mbingu kwa ajili yako wewe binafsi. Wewe ni muhimu Kwake.

**15. Je, ufalme huu unatayarishwa kwa ajili yangu binafsi?**
"Yeyote anayetaka, na ayatwae maji ya uzima bure." Ufunuo 22:17 . "Kwa urithi usioharibika ... uliohifadhiwa mbinguni kwa ajili yenu." 1 Petro 1:4. "Naenda kuwaandalia mahali." Yohana 14:2.

**Jibu: Ndiyo, Mbingu** Imetayarishwa kwa ajili yako binafsi. Mwaliko kutoka kwa Bwana ni kwako wewe binafsi. Ukikataliwa kuingia huko rafiki, hutakuwa na wa kumlaumu isipokuwa wewe mwenyewe.

Yesu anapoishi ndani ya mioyo yetu na kukaa katika nyumba zetu, tunahakikishiwa nafasi katika ufalme Wake wa mbinguni.

**16. Ninawezaje kuhakikishiwa mahali katika ufalme huo mkuu na mtukufu?**
"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia." Ufunuo 3:20. "Heri wazishikao amri Zake, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake." Ufunuo 22:14 . "Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni." Mathayo 7:21 . "Wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu." Yohana 1:12. "Damu ya Yesu Kristo Mwana Wake yatusafisha dhambi yote." 1 Yohana 1:7 .

**Jibu:** Biblia inaiweka wazi. Ni rahisi. Mpe Kristo maisha yako kwa utakaso wa dhambi. Unapofanya hivi, anakupa pia uwezo wa kufanya mapenzi Yake na kushika amri Zake. Hii ina maana, bila shaka, kwamba utaanza kuishi kama Kristo aliishi na utashinda dhambi zote. "Yeye ashindaye atayarithi yote." Ufunuo 21:7 . Kwa ufupi, mtu huandaliwa kwa ajili ya mbinguni wakati ana mbingu moyoni mwake.

**17. Nimeamua kukubali toleo la Yesu la kuishi naye milele katika ufalme Wake wa mbinguni.**
**Jibu:**

# Maswali ya Kutafakari

**1. Mbingu inawezaje kuwa mahali pa furaha wakati waliookolewa wanawafikiria wapendwa wao waliopotea?**
Biblia inasema kwamba Mungu “atafuta machozi yote kutoka katika macho yao.” Ufunuo 21:4 . Wakiwa wamezungukwa na uzuri na shangwe za dunia mpya, watu wa Mungu waliokombolewa watasahau majanga na maumivu ya moyo ya wakati uliopita; “ya kwanza hayatakumbukwa, wala hayataingia moyoni.” Isaya 65:17 .

**2. Biblia inasema, “Nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu.” 1 Wakorintho 15:50. Basi, waliokombolewa wanawezaje kuwa nyama na mifupa?**
Hapa Biblia inatumia neno “mwili” kufafanua mtu ambaye hajaongoka. Wazo kama hilo laelezwa katika Warumi 8:8 , 9 : “Wale waufuataao mwili hawawezi kumpendeza Mungu. Yohana 3:6 inasema, “Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho.” Neno “mwili” hapa tena linamaanisha mtu ambaye hajaongoka, wakati neno “roho” linamaanisha mtu aliyeongoka au “aliyezaliwa mara ya pili”. Kwa hiyo Biblia inasema tu katika 1 Wakorintho 15:50 kwamba hakuna mtu awezaye kuingia katika ufalme wa Mungu isipokuwa uongofu ufanyike kwanza na mwili kuwa roho. Kristo, katika mwili wake uliofufuka, alitangaza kwamba alikuwa kweli “mwili na mifupa.” Luka 24:39 . Tutakuwa na mwili kama Wake, kulingana na Wafilipi 3:21 .

**3. Je, mtume Petro ndiye anayesimamia lango la jiji takatifu?**
Hapana! Biblia inasema katika Ufunuo 21:12 kwamba Yerusalemu mpya - mji mtakatifu wa Mungu - ina milango 12, na kwenye malango malaika 12. Hakuna rejelea inayofanywa katika Biblia kwa mtume yeyote kuwa mlinzi wa malango.

**4. Je, mji mtakatifu Kweli ni mkubwa kiasi cha kuwachukua watu wote waliookoka wa nyakati zote?**
Ikiwa jiji lingekuwa na watu wengi na kila mtu aliyeokolewa apewe eneo la futi za mraba 100 tu, Je, kungekuwa na nafasi kwa watu bilioni 39 katika jiji hilo, ambalo ni mara nyingi zaidi ya idadi ya watu ulimwenguni. Wataalamu wengi wa takwimu wanaamini kwamba ikiwa watu wote ambao wamewahi kuishi wangeokolewa, kungekuwa na nafasi nyingi kwa ajili yao katika jiji. Maandiko yanaweka wazi, hata hivyo, kwamba ni wachache tu watakaookolewa ( Mathayo 7:14 ). Kwa hivyo kutakuwa na nafasi zaidi ya kutosha katika jiji kubwa.

**5. Wakati mwingine mimi hujiuliza kama thawabu ina thamani ya kujitoa kote ambako kumefanyika. Inaonekana kwamba Shetani anakaribia kunishinda nyakati fulani. Je, Biblia hunitia moyo?**
Ndiyo. Kwa kweli, lazima mtume Paulo alikuwa akimfikiria mtu kama wewe alipoandika, “Mateso ya wakati huu wa sasa hayastahili kulinganishwa na utukufu utakaofunuliwa ndani yetu. Warumi 8:18 . Mtazamo mmoja tu wa ufalme huo wa milele utasababisha majaribu na mateso mabaya zaidi ya dunia kuwa duni, na waliokombolewa watapaza sauti: “Haleluya, mbingu ina gharama nafuu vya

kutosha kuifikia!”

**6. Je! watoto wadogo wanaokufa wataokolewa katika ufalme wa Mungu?**
Hatuna jibu hususani la Biblia kwa swali hili, lakini wengi huchagua kuamini kwamba watoto wachanga wataokolewa kwa msingi wa Mathayo 2:16-18 . Hapo Biblia husema juu ya mfalme mwovu Herode akiwaua watoto wachanga wote wa kiume katika Bethlehemu waliokuwa na umri wa miaka miwili au chini ya hapo. Agano la Kale lilitabiri tukio hili la kutisha na la kikatili, na Mungu akawaambia akina mama waache kulia kwa sababu watoto wao siku moja watarudishwa kwao. “Zuia sauti yako usilie, ... [watoto waliouawa] Maana kazi yako itapata thawabu, nao watakuja tena toka nchi ya adui; Ndivyo asemavyo Bwana. Tena liko tumaini kwa siku zako za mwisho, asema Bwana; na watoto wako watarejea hata mpaka wao wenyewe..” Yeremia 31:16 , 17 . Hii ni kumbukumbu ya wazi ya ufufuo.

**7. Je, ninaelewa kwa usahihi kwamba mbingu, makao ya waliookolewa, yatakuwa hapa duniani?**
Hiyo ni sahihi. Ingawa mji mtakatifu sasa uko katika makao ya Mungu, Yeye atauhamisha hapa duniani. Dhambi na wenye dhambi wataangamizwa kwa moto, na dunia itafanywa kuwa mpya na kupewa wenye haki katika utukufu na uzuri wake wote wa Edeni. Jiji takatifu litakuwa jiji kuu la dunia mpya, na Mungu atakihamishia kiti Chake cha enzi hapa ( Ufunuo 21:2 , 3 ; 22:1 , 3 ) na kuishi pamoja na waadilifu papa hapa duniani kote kwa umilele. Na akaapo Bwana, ndipo mbingu ilipo. Mpango wa Mungu ni kumrudishia mwanadamu kile ambacho Adamu alipoteza: utukufu wa maisha makamilifu kwenye sayari kamilifu. Shetani na dhambi zilikatiza mpango wa Mungu, lakini mpango huo utatekelezwa. Sote tunaweza kushiriki katika ufalme huu mpya--na ni lazima tuwepo huko jamani! Kwani ina mambo mengi mazuri nasi hatupaswi kukosa hata tone la mambo hayo mazuri.

**8. Kwa nini wengi hufundisha na kuamini kwamba nyumba ya waliookolewa ni mahali penye ukungu na wakaaji kama mizimu au roho wanaoelea juu ya mawingu na hawafanyi lolote ila kucheza vinubi?**

Mafundisho haya yalitoka kwa ibilisi, baba wa uongo ( Yohana 8:44 ). Anatamani kupotosha mpango wa upendo wa Mungu na kuwasilisha mbingu kama sehemu isiyo halisi, “yenye mambo ya ushirikina fulani” ili watu wapoteze matamanio au kuwa na mashaka juu ya Neno la Mungu kabisa. Shetani anajua vema kwamba wanaume na wanawake wanapoelewa kikamilifu zile kweli za Biblia kuhusu makazi ya waliookolewa, nguvu zake juu yao zitaondoka, kwa sababu wataanza kufanya mkakati wa kuingia katika ufalme huo wa mbinguni. Hii ndiyo sababu anajitahidi sana kuficha suala hilo na kueneza uwongo kuhusu makao hayo ya mbinguni.

# Maswali ya Chemsha Bongo Kwizz

**1. Mji mtakatifu ulio angani (1)**

_____ Si halisi, bali ni mfano tu.
_____ Je, ni mji halisi unaotayarishwa sasa na Mungu katika makao yake.
_____ Haupo isipokuwa katika mawazo ya baadhi ya watu.

**2. Mji huu mtakatifu (1)**
_____ Utaharibiwa na mlipuko wa nyuklia.
_____ Utakamatwa na Shetani na jeshi lake.
_____ Utashuka katika dunia hii na kuwa makao makuu ya dunia kufanywa mpya.

**3. Katika orodha ifuatayo, angalia Ukweli halisi wa Biblia kuhusu mji mtakatifu: (7)**
_____ Unaitwa Yerusalemu mpya.
_____ Ni sawa na ukubwa wa London.
_____ Kuta zake ni madini ya topazi.
_____ Mji ni mraba, urefu ni kama upana wake.
_____ Barabara ni za dhahabu safi.
_____ Mji una misingi 14.
_____ Mtume Petro anasimama kwenye lango lake.
_____ Kila mmoja ya milango yake 12 imetengenezwa kwa lulu moja.
_____ Mzingo wake ni maili 1,500.
_____ Misingi yake yote imetengenezwa kwa mawe ya thamani.
_____ Jiji litakuwa katika uwiano kamili.

**4. Mti wa uzima (1)**
_____ Ni mti halisi ambao utawapa watu wa Mungu nguvu na ujana wa milele.
_____ Ni tamathali ya usemi na inamaanisha kwamba Mungu atawapa watu Wake nguvu.
_____ Ulikuwepo hapo mwanzo lakini hautajumuishwa katika ufalme wa dunia mpya.

**5. Katika orodha ifuatayo, angalia vitu vyote ambavyo ni ahadi za Kweli za Biblia kwa watu katika ufalme mpya wa Mungu: (5)**
_____ Bwana atafunga ndoa kila siku.
_____ Mti wa uzima huzaa aina 20 za matunda.
_____ Bwana mwenyewe ataishi pamoja na watu Wake.
_____ Baada ya miaka milioni, watakatifu watakuwa wameboeka/wachoka.
_____ Hakutakuwa na kifo wala huzuni tena.
_____ Watu hawatachoka kamwe.
_____ Viwete watabebwa na malaika.
_____ Malaika watakuwa madaktari na kufanya shughuli zote.
_____ Vipofu watapata kuona.

_____ Wivu, woga, chuki, uwongo, husuda, uchafu n.k. vitatoweka milele.
_____ Watoto hawatakua.

**6. Angalia kauli hapa chini zinazosema Ukweli kuhusu dunia mpya: (6)**
_____ Bahari za leo hazitakuwapo tena.
_____ Majangwa yatakuwa makubwa zaidi.
_____ Wanyama watahifadhiwa katika vizimba vya kupendeza vya mbinguni.
_____ Vimbunga, matetemeko ya ardhi, na mafuriko hayatajulikana.
_____ Vipande vya sigara vitaondolewa kwa uangalifu kutoka mitaani kila siku na malaika.
_____ Maua na miti haitanyauka au kufifia.
_____ Mbingu itakuwa hapa duniani.
_____ Dhambi haitatokea mara ya pili.
_____ Utukufu wa yote hauwezi kuelezewa.

**7. Wenye haki katika ufalme wa mbinguni (1)**
_____ Watakuwa roho au mizimu wanaopiga vinubi na kuelea juu ya mawingu.
_____ Sitawatambua wapendwa na marafiki wengine ambao wanaweza kuwa huko.
_____ Watu watakuwa na miili halisi ya nyama na mifupa na watajuana.

**8. Tunajua kwamba watu mbinguni watakuwa halisi na watafanya mambo halisi kwa sababu (1)**
_____ Sayansi imethibitisha hili kwa ukamilifu.
_____ Biblia inasema tutakuwa kama Kristo, ambaye alikuwa halisi (alikuwa na nyama na mifupa) baada ya kufufuka Kwake na kufanya mambo halisi
_____ Wahubiri wengi husemaga hivyo.

**9. Ninaweza kuwa na uhakika wa mahali katika ufalme huo wa mbinguni ikiwa (1)**
_____ Ninasema kila siku kwamba ninampenda Bwana.
_____ Ninaogopa vya kutosha kuzimu/Jehanamu.
_____ Namkubali na kumfuata Kristo na kuzishika amri Zake.

**10. Watu waliookolewa watafanya nini katika ufalme wa mbinguni? Angalia Ukweli wa zile Kweli za Biblia zilioorodheshwa hapa chini: (5)**
_____ Watajenga nyumba na uishi humo.
_____ Watapanda mizabibu.
_____ Wataua wanyama na kuwala.
_____ Watapiga ala za mbinguni na kumwimbia Mungu sifa.
_____ Wataabudu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu.
_____ Wataruka kuzimu na kuwadhihaki waliopotea.
_____ Watakula matunda ya mti wa uzima.

# Funguo za Ndoa yenye Furaha

**Somo la 5**

Pengine umesikia kwamba karibu nusu ya ndoa zote sasa huishia kwenye talaka, na kuacha wenzi wenye uchungu na watoto waliochanganyikiwa. Usiruhusu hili likufanyikie! Ikiwa ndoa yako inapitia nyakati ngumu au ni ndoa yenye furaha, au hata kama bado hujaolewa, ukizingatia haya, hapa kuna ushauri wa bure lakini uliothibitishwa wa kusaidia ndoa yako kudumu.

Ushauri huu ni moja kwa moja kutoka kwa Mungu, aliyeumba na kupanga ndoa! Ikiwa umejaribu kila kitu kingine, kwa nini usimpe Mungu nafasi? Fuata funguo katika mwongozo huu, na unaweza kulinda nyumba yako.

## Kanuni Kumi na Saba za Ndoa yenye Furaha Kutoka katika Kitabu Kikubwa cha Mungu

Anza kwa kukaa nyumbani mwako mwenyewe, hata ikiwa ni lazima ukae katika chumba kimoja.

### 1. Anzisha nyumba yako ya kibinafsi.

"Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja." Mwanzo 2:24 .

**Jibu:** Utawala wa Mungu ni hususani. Wenzi wa ndoa wanapaswa kuwaacha baba na mama na kuanzisha nyumba yao wenyewe, hata ikiwa fedha zinahitaji kuwa na chumba kimoja. Mume na mke wanapaswa kuamua pamoja kuhusu sera kama hizi. Kisha mwanamume awajulishe jamaa zake na yeye mwanamke pia. Ni lazima wabaki imara bila kujali nani anapinga. Maelfu ya talaka zingeepukwa ikiwa sheria hii ingefuatwa kwa uangalifu.

Usisahau kwamba Mungu Mwenyewe Ndiye aliyekuunganisha katika ndoa. Ni taasisi ya ubunifu wa Mungu. Na Ndiye sheria Zake katika ndoa zinapaswa kufuatwa.

### 2. Endelea uchumba wako.

"Zaidi ya yote shikaneni upendo usiopungua ninyi kwa ninyi, kwa kuwa upendo husitiri wingi wa dhambi." 1 Petro 4:8 , RSV.* "Mumewe ... humsifu." Mithali 31:28 . "Yeye aliyeolewa hujishughulisha ... jinsi atakavyompendeza mumewe." 1 Wakorintho 7:34 . "Iweni na upendo mzuri ninyi kwa ninyi ... kwa heshima mkipendelea zaidi ninyi kwa ninyi." Warumi 12:10 .

**Jibu:** Endelea (au labda ufufue) adabu na staha za uchumba katika maisha yako ya ndoa. Ndoa zenye mafanikio hazitokei tu kimiujiza, bali ni lazima ziendelezwe na

kupapaliwa haswa. Msichukuliane kuwa kwa ukawaida tu, kwamba huyu ni wangu wa yuko tu hapa nyumbani na nitamkuta tu ataenda wapi, utaharibu mambo au ukiritimba utakaotokea utaharibu ndoa yenu. Mchukulie mwenzi wako kama mtu spesheli. Endeleni kukua katika upendo kwa kuonyeshana kujaliana, la sivyo huo upendo utakufa, au utasambaratika. Kila mmoja amjali mwingine na kuishi kwa kutunza miahadi (commitment). Upendo na furaha havipatikani kwa kutafuta ili upate kwaajili yako mwenyewe tu, bali kwa kuwapa wengine pia. Kwa hiyo tumia wakati mwingi kadri iwezekanavyo kufanya mambo pamoja ikiwa mtaelewana vizuri. Jifunzeni kusalimiana kwa shauku. Tumieni likizo, tembeleaneni, nendeni sokoni pamoja, mfanye utalii pamoja, kuleni pamoja, vyote hivi ni vyema kuvifanya mkiwa katika vikundi au marafiki wengine kujiepushe na majaribu na kuepuka mwonekano wa uovu. Msipuuzie kufanyiana mambo madogomadogo, kutiana moyo, na matendo ya ukarimu au upendo. Mshangaze mwenzako kwa zawadi ndogo au upendeleo fulani. Jaribu “kumzidi mwenzako katika kumpenda”. Usichote mema mengi kutoka kwenye ndoa kuliko unavyoweka ndani yake. Talaka yenyewe sio mharibifu mkubwa wa ndoa, lakini badala yake, ni ukosefu wa upendo. Ukipewa nafasi, upendo daima hushinda.

Mshangaze mwenzako kwa zawadi ndogo.

**3. Kumbuka kwamba Mungu alikuunganisha pamoja katika ndoa.**

“Kwa sababu hiyo mwanamume atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe. ...Kwa hiyo si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe.” Mathayo 19:5 , 6 .

**Jibu: Je!** upendo umekaribia kutoweka nyumbani kwako? Ibilisi (ndiyo mvunja nyumba mashuhuri) anahusika na hili. Usisahau kwamba Mungu Mwenyewe aliwaunganisha pamoja katika ndoa, na anakusudia mkae pamoja na kuwa na furaha. Yeye Ataleta furaha na upendo maishani mwako ikiwa utatii sheria Zake za Mbinguni (amri). “Kwa Mungu yote yanawezekana.” Mathayo 19:26 . Usikate tamaa. Mungu, ambaye huweka upendo moyoni mwa mmisionari kwaajili ya mwenye ukoma ambaye ni mpagani, anaweza kukupa upendo kwa urahisi ikiwa utamruhusu.

Mawazo yasiyofaa yanaweza kuharibu ndoa yako.

**4. Linda mawazo yako--usiruhusu hisia zako zikunase.**

“Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo.” Mithali 23:7 . “Usimtamani mke wa jirani yako.” Kutoka 20:17 . “Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; maana ndiko zitokako chemchemi za uzima.” Mithali 4:23 . “Mambo yoyote yaliyo ya kweli, ... ya uaminifu, ... ya haki, ... safi, ... ya kupendeza, ... yenye ripoti nzuri; ... fikiria juu ya mambo haya.” Wafilipi 4:8 .

**Jibu:** Mawazo yasiyofaa yataharibu ndoa yako. Ibilisi atakutega kwa mawazo kama haya: “Ndoa yetu ilikuwa kosa.” “Hanielewi.” “Siwezi kuchukua mengi zaidi ya hii.” “Tunaweza talaka kila wakati ikiwa ni lazima.” “Nitaenda nyumbani kwa mama.” “Alitabasamu mwanamke yule.” Acha kuwaza mawazo kama haya au

ndoa yako imekwisha, kwa sababu mawazo yako na hisia zako hutawala matendo yako. Epuka kuona, kusema, kusoma, au kusikia chochote ambacho (au kujihusisha na mtu yeyote ambaye) kinapendekeza uchafu au kutokuwa mwaminifu. Mawazo yasiyodhibitiwa ni kama gari lisilo na breki kwenye mlima. Chochote kinaweza kutokea, na matokeo yake daima ni maafa.

**5. Kamwe usiende kupumzika usiku ukiwa kwa mwenzako.**

"Jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka." Waefeso 4:26 . "Ungameni makosa yenu ninyi kwa ninyi." Yakobo 5:16 . "Kusahau yale yaliyo nyuma." Wafilipi 3:13 . "Iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi." Waefeso 4:32 .

**Jibu:** Kukasirika na kuwa na jazba juu ya maudhi na manung'uniko (makubwa au madogo) ni hatari sana. Isipokuwa yatatatuliwa haraka, hata yale matatizo madogo huwekwa akilini mwako huku imani na mitazamo yako ikiendelea kuathiri vibaya falsafa yako yote ya maisha. Hii ndiyo sababu Mungu anasema tuache hasira ipoe kabla ya kulala usiku. Uwe umepevuka akili vya kutosha kusamehe na kusema kwa uaminifu, "Samahani." Baada ya yote, hakuna mtu mkamilifu, na kumbuka kuwa nyote mko kwenye timu moja, kwa hivyo kuwa mchezaji mzuri kwa kadri inavyowezekana kwa kukubali kosa unapolifanya. Mbali na kwamba kutengeneza ndoa iwe nzuri ni jambo lenye uzoefu wa kupendeza sana, na lenye nguvu zisizo za kawaida za kuwavuta wenzi wa ndoa karibu zaidi. Mungu anapendekeza ufanye hivyo! Na kila nachokipendekeza hufanya kazi!

Ukiwa na Kristo ndani ya moyo na nyumba yako, ndoa yenu itafanikiwa.

**6. Mweke Kristo kiini au kitovu cha nyumba yako.**

"Bwana asipoijenga nyumba, waijengao wafanya kazi bure." Zaburi 127:1 . "Katika njia zako zote mkiri Yeye, Naye atayanyosha mapito yako." Mithali 3:6 . "Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu." Wafilipi 4:7 .

**Jibu:** Hii ndiyo kanuni kubwa kabisa. Kwa kweli inashughulikia kuliko zingine zote. Mweke Kristo kwanza! Siri ya kweli ya furaha ya kweli ndani ya nyumba si diplomasia, mkakati, na jitihada zisizochoka za kushinda matatizo, bali ni kuungana na Kristo, ni kuwa na ubia Naye. Mioyo iliyojaa upendo wa Kristo kamwe haiwezi kuwa mbali sana kutoka kwa mwingine. Kristo akiwa nyumbani, ndoa itafanikiwa. Injili ndiyo tiba ya ndoa zote zilizojaa chuki, uchungu na kukatishwa tamaa. Injili inazuia maelfu ya talaka kwa kurejesha upendo na furaha kimuujiza. Mwenyezi Mungu ataokoa ndoa yako, ikiwa uko tayari.

Ombeana kwa sauti.

**7. Ombeni pamoja.**

"Ombeni, ili msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu." Mathayo 26:41 . "Ombeni mmoja kwa mwingine." Yakobo 5:16 . "Lakini mtu wa

kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu.” Yakobo 1:5 .

**Jibu:** Ombeni kwa sauti! Huu ni utawala wa ajabu ambao unafanikiwa zaidi ya ndoto kali zaidi. Pigeni magoti mbele za Mungu na mwombeni kwa ajili ya upendo wa Kweli ninyi kwa ninyi, kwa msamaha, kwa nguvu, kwa hekima--kwa ajili ya ufumbuzi wa matatizo. Mungu ametoa hakikisho la kibinafsi kwamba atajibu. Mwenye kusali haponywi moja kwa moja kutoka kwa makosa yake yote, bali atakuwa na moyo unaotaka kutenda haki. Hakuna familia inayovunjika huku ikisali pamoja kwa unyoofu ili kupata msaada wa Mungu. Utafiti wa kanisa la Baptisti ulionyesha kwamba japo marekani asilimia hamsini za ndoa huvunjika, ndoa za waumini wanaoomba pamoja asubuhi na jioni, maombi ya dhati, bila unafiki na kuwa wakweli moyoni, ni ndoa moja tu kati ya 1023 ndiyo huvunjika!

Msamaha siku zote ni bora kuliko talaka.

### 8. Kubali kwamba talaka si jibu.

“Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe.” Mathayo 19:6 . “Kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa ajili ya uasherati, na kuoa mwingine, azini; Mathayo 19:9 . “Mwanamke aliye na mume amefungwa na sheria kwa mume wakati yu hai.” Warumi 7:2.

**Jibu:** Biblia iko wazi. Mahusiano ya ndoa yanakusudiwa kuwa yasiyoweza kufutwa na yasiyoweza kuharibika. Talaka inaruhusiwa tu katika kesi ya zinaa. Lakini hata hivyo siyo lazima muachane, umeruhusiwa, ila jitahidini kuokoa ndoa yenu kwa kadri inavyowezekana. Mifano ya Biblia inaweza kutueleza zaidi hili. Msamaha daima ni bora kuliko talaka, hata katika kesi za kuanguka kwa maadili. Ndoa ni jambo la maisha yote. Mungu aliamuru hivyo wakati alipofanya harusi ya kwanza katika Edeni. Mawazo ya talaka kama suluhu yataharibu ndoa yoyote. Hii ndoup sababu moja ya Yesu kukataa kuachana. Talaka daima ni uharibifu na karibu wakati wote si suluhisho la tatizo. Badala yake, husababisha matatizo makubwa zaidi, kwa hiyo haipaswi kamwe kuzingatiwa moyoni. Maisha yaliyo na mpasuko, yaliyokatishwa tamaa, yasiyo na furaha na yaliyopotoka karibu wakati wote yanaifuata talaka, na hata mafanikio katika maisha yenyewe mara nyingi huzuiwa. Mungu alianzisha ndoa ili kulinda usafi na furaha ya watu, kuwaandalia mahitaji yao ya kijamii, na kuinua hali yao ya kimwili, kiakili, na kiadili. Nadhiri Zake ni miongoni mwa ahadi nzito ambazo humfunga mwanadamu kuliko zingine zote. Kuziweka kando kirahisi hupelekea mtu kujiondoa katika kibali na baraka za Mungu.

### 9. Weka mzunguko wa familia ulio karibu.

“Usizini.” Kutoka 20:14 . “Moyo wa mumewe humwamini salama. ... Atamfanyia mema wala si mabaya siku zote za maisha yake.” Methali 31:11 , 12 . “Bwana amekuwa shahidi kati yako na mke wa ujana wako, ambaye umemtenda kwa hiana.” Malaki 2:14 . “Jilinde na mwanamke mwovu .... Usiutamani uzuri wake moyoni mwako, wala asikushike kwa kope zake .... Je! . Ndivyo aingiaye kwa mke wa jirani yake; kila amgusaye atakuwa hana hatia.” Mithali 6:24-29 .

**Jibu:** Mapenzi na ukaribu wa kifamilia haupaswi kamwe kushirikiwa na wengine--hata na wazazi washirikishwe ikibidi sana. Ni dhambi na msiba mkubwa kuvunja sheria hii tuliyopewa na Mungu. Mtu wa tatu wa kuhurumia au kusikiliza malalamiko ni chombo cha shetani cha kutenganisha mioyo ya mume na mke. Tatua matatizo yako ya nyumbani kwa faragha. Hakuna mtu mwingine (isipokuwa mchungaji wako au mshauri wa ndoa) anayepaswa kuhusika. Daima muwe wakweli kwa kila mmoja, na kamwe msifiche siri kutoka kwa kila mmoja. Usiseme utani kwa gharama ya hisia za mwenzi wako. Mlindane kwa nguvu, na kuwatenga kabisa wavamizi wote. Na kuhusu uzinzi (licha ya yale ambayo baadhi ya washauri wa ndoa wanasema), sikuzote unakuumiza wewe na wengine wote wanaohusika. Mungu, ambaye anajua akili zetu, mwili, na muundo wa hisia (na anajua nini hutusaidia au kutuumiza) ametoa katazo, "Usifanye." Na anaposema, "Usizini," ni afadhali tusifanye. Wale wanaopuuza utawala Wake watalipa adhabu kuu. Kwa hivyo ikiwa kuchangamkia mtu wa jinsia nyingine au kutongozana kumeanza, vunja jambo hilo mara moja, au vivuli vinaweza kutulia juu ya maisha yako ambavyo haviwezi kuinuliwa.

Kwa upendo wa kweli, ndoa yako haiwezi kushindwa.

**10. Mungu anaelezea upendo, fanya kuwa lengo lako la kila siku kujipima kwa haya mafungu.**

" Upendo huvumilia, upendo hufadhili; upendo hauna wivu au majivuno. Upendo hauna kiburi na haukosi kuwa na adabu. Upendo hau tafuti kujipendeza nafsi; haukasiriki upesi, hauweki orodha ya mabaya. Upendo haufurahii mabaya, bali hufurahia kweli. Upendo huvumilia yote, huamini yote, hutumaini yote, hustahim ili yote.

"1 Wakorintho 13:4-7"

**Jibu:** Tafadhali soma tena mafungu ya Maandiko hapo juu kwa makini. Haya ndiyo maelezo ya Kweli ya Mungu kuhusu upendo. Je, unajipima vipi? Upendo sio msukumo wa hisia, lakini kanuni takatifu inayohusisha kila awamu na hatua ya maisha. Kwa upendo wa kweli, ndoa yako haiwezi kushindwa. Bila huo upendo wa kweli, haiwezi kufanikiwa.

Jaribu kumfurahisha mwenzi wako, badala ya kuwa mzuri.

**11. Kumbuka kwamba kukosoa na kukashifu huharibu upendo.**

"Enyi waume, wapendeni wake zenu, wala msiwe na uchungu juu yao." Wakolosai 3:19 . "Heri kukaa nyikani kuliko kukaa pamoja na mwanamke mgomvi na mwenye hasira." Mithali 21:19 . "Mke mgomvi ni kama matone yasiyokoma ya siku ya mvua" Mithali 27:15 . "Mbona wakitazama kibanzi kilicho katika jicho la ndugu yako, lakini huiangalii boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe?" Mathayo 7:3 . "Upendo ... hutafuta njia ya kujenga." 1 Wakorintho 13:4

**Jibu:** Acha kukosoa, kugombana, na kutafuta makosa. Mume au mke wako anaweza kukosa mengi, lakini kugombana hakutasaidia. Usitarajie ukamilifu, vinginevyo uchungu utatokea. Usiyafikirie makosa, bali wewe yawinde yale mambo

mema. Usijaribu kurekebisha, kudhibiti, au kulmazimisha mpenzi wako kufanya jambo, utaharibu upendo. Mungu pekee Ndiye anayeweza kubadilisha watu. Hali ya ucheshi, moyo mkunjufu, fadhili, subira, na mapenzi vitaondoa thuluthi mbili ya matatizo yako ya ndoa. Jaribu kumfanya mwenzi wako awe na furaha kuliko kujizikia vizuri, na mambo mazuri yatajileta yenyewe. Siri ya ndoa yenye mafanikio sio kuwa na mwenza sahihi, bali ni kuwa mwenzi sahihi.

Jifunze kucheka na kufurahia nyakati zinazofaa pamoja.

**12. Usipitilize katika jambo lolote, uwe na kiasi.**

"Kila mtu ashindanaye ana kiasi katika mambo yote." 1 Wakorintho 9:25 . "Upendo ... haufuati faida za ubinafsi." 1 Wakorintho 13:5 , "Basi mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu." 1 Wakorintho 10:31 . "Nauweka chini ya mwili wangu, na kuutia katika utumwa." 1 Wakorintho 9:27 . "Ikiwa yeyote hatafanya kazi, basi asile." 2 Wathesalonike 3:10 . "Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi." Waebrania 13:4 . "Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake. Wala msivitoe viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi." Waroma 6:12 , 13 .

**Jibu:** Kufanya mambo kwa kupita kiasi kutaharibu ndoa yako. Vivyo hivyo kutofanya kutaleta shida. Kazi, upendo, mapumziko, mazoezi, michezo, ibada, milo, na mawasiliano ya kijamii lazima yawe na msawaziko/balansi katika ndoa yako, au jambo fulani litatokea. Kufanya kazi kupita kiasi na kukosa usingizi, kukosa chakula kinachofaa, au mazoezi humfanya mtu kuwa mkosoaji, asiyestahimili, na asiyefaa. Kula kupita kiasi mara kwa mara ni uovu mkubwa ambao huimarisha asili ya tabia za kwenda chini na hufanya dhamiri ya mtu iwe butu.

Unyanyasaji wa kijinsia au ngono inayopitiliza huharibu kupenda vitu vitakatifu na kudhoofisha uhai. Ndoa haitoi ruhusa ya kufanya ngono kupita kiasi. Matendo ya ngono yenye kushusha hadhi, yaliyopotoka, au yasiyo na kiasi huharibu upendo na heshima kati yenu. Maisha ya ngono ya wastani yanapendekezwa na Biblia na yatalinda afya zenu mpaka uzeeni. ( 1 Wakorintho 7:3-7 ). Mawasiliano ya kijamii na wengine ni muhimu kabisa. Furaha ya kweli haiwezi kupatikana kwa kujitenga. Ni lazima tujifunze kucheka na kufurahia nyakati nzuri na bora. Kuwa makini kupita kiasi ni hatari ( too serious). Kutenda kupita kiasi au kutofanya jambo lolote kunadhoofisha akili, mwili, dhamiri, na uwezo wa kupendana na kuheshimiana. Usiruhusu kutokuwa na kiasi kuharibu ndoa yako.

Usiangalie mkomba/pochi ya mwingine au mali yake binafsi bila ruhusa.

**13. Heshimu haki za kibinafsi na upekee wa kila mmoja.**

"Upendo hustahimili. ... Upendo haujui wivu. ... haukosi adabu, hautafuti kujipendeza nafsi. ... Hafurahii dhuluma. ... umejaa uaminifu." 1 Wakorintho 13:4-7a , "Iweni na upendo wenye fadhili ninyi kwa ninyi kwa upendo wa kindugu; Warumi 12:10 .

**Jibu:** Kila mwenzi ana haki aliyopewa na Mungu ya faragha fulani bila ya kutoa

maelezo. Usichezee pochi au mikoba ya kila mmoja, barua binafsi na mali nyingine za binafsi isipokuwa upewe ruhusa. Haki ya faragha na utulivu inapaswa kuheshimiwa. Mume au mke wako ana haki ya kukosea sehemu ya muda na ana haki ya kuwa na siku y a "off" bila kupigiwa kipenga. Wenzi wa ndoa hawamilikiani na hawapaswi kamwe kujaribu kulazimisha mabadiliko ya haiba ya mwingine.

Ni Mungu pekee Yake, Ndiye anayeweza kufanya mabadiliko hayo, na kila mmoja wetu atajibu mwenyewe Kwake kuhusu jambo hili ( Warumi 14:12 ). Kumwamini mwingine kikamilifu na kuaminiana, bila ya kushukiana au kupeleleza mambo au kusachi vitu vya mwingine, ni muhimu kabisa kwa furaha. Kila mmoja kwa asilimia 100 awajibike kwa Mungu. Yeye anapeleleza moyo na hatuwezi kuwa feki Kwake. Uwe Mkweli kwa Mungu, na kutaka kuboresha ndoa yako kwa uwezo wako wote, ukimtii Mungu kwanza. Tumia muda kidogo kujaribu "kumjua" mwenzi wako na muda mwingi kujaribu kumfurahisha. Hii itafanya maajabu.

Nyumba safi na yenye utaratibu hutatua matatizo mengi ya familia.

**14. Uwe safi, mwenye kiasi, mwenye utaratibu, na mchaji.**

"Vivyo hivyo wanawake wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri." 1 Timotheo 2:9 . "Yeye ... anafanya kazi kwa mikono ya hiari." "Huamka bado usiku na kuwaandalia watu wa nyumbani mwake chakula." "Huangalia sana njia za watu wa nyumbani mwake, wala hali chakula cha uvivu." Mithali 31:13 , 15 , 27 , "Iweni safi." Isaya 52:11 . "Mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu." 1 Wakorintho 14:40 . "Ikiwa mtu hatunzi ... wale wa nyumbani mwake, ameikana imani, na ni mbaya zaidi kuliko kafiri." 1 Timotheo 5:8 . "Usiwe mvivu." Waebrania 6:12 .

**Jibu:** Uvivu, fujo, uchafu, na uzembe ni silaha za shetani za kuharibu heshima na mapenzi yenu ninyi kwa ninyi, na hivyo kuharibu ndoa yenu. Mavazi nadhifu, yenye kiasi na miili safi, iliyopambwa vizuri ni muhimu kwa mume na mke. Milo inapaswa kuwa mizuri, yenye kukimu uwezo wenu wa pesa, yenye kuvutia, na kutolewa kwa wakati. Nyumba inapaswa kuwa safi na yenye utaratibu, kwa sababu hilo huleta amani, utulivu, na moyo kuridhika. Mume mvivu, asiye na mabadiliko na asiyeitunza nyumba yake ni laana kwa familia yake na ni dharau kwa Mungu. Kutokujali katika baadhi ya mambo haya kunaonekana kuwa kudogo ila kunaharibu nyumba maelfu.

Maneno makali na yenye hasira huvunja hamu ya mwenzi wako ya kutaka kukufurahisha.

**15. Azimia kuzungumza kwa upole, kwa fadhili na kwa njia laini/nyororo.**

"Jawabu la upole hugeuza hasira; Bali maneno makali huchochea hasira." Mithali 15:1 . "Ishi kwa furaha na mke unayempenda." Mhubiri 9:9 . "Nilipokuwa mwanamume, niliacha mambo ya kitoto." 1 Wakorintho 13:11 .

**Jibu:** Jilazimishe kuzungumza kwa upole na fadhila kwa mwenzi wako. Ukimya, mtu anaposhambuliwa, mara nyingi ndiyo njia bora ya kutuliza hasira. Maamuzi

yanayofanywa ukiwa na hasira, uchovu au kuvunjika moyo hayategemeki hata hivyo, kwa hivyo ni bora kupumzika na kuacha hasira ipoe. Na unapozungumza, basi iwe daima ni kwa utulivu na kwa upendo. Maneno makali na yenye hasira husagasaga hamu ya mwenzi wako ya kutaka kukufurahisha.

Kujadili na kukubaliana katika masuala ya fedha.

**16. Awe mwenye busara katika mambo ya pesa.**

"[Upendo] haumiliki. ... Upendo haukosi kuwa na adabu na haufuati kujipendeza nafsi." 1 Wakorintho 13:4 , 5 . "Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu." 2 Wakorintho 9:7 .

**Jibu:** Mali na mapato yote katika ndoa yanapaswa kuwa "yetu," sio "yako" na "yangu." Wake ambao hawafanyi kazi nje ya nyumba wanapaswa kupokea kiasi cha pesa kila mwezi kwa kununua chakula, nguo, na vitu vingine vilivyowekwa kwenye bajeti. Pesa hii inapaswa kutolewa kwa furaha badala ya kutolewa kwa kinyongo na roho y amagomvi. Mke na mume wote wanapaswa kuwa na kiasi kidogo cha pesa sawa (inapowezekana) kutumia kama wanavyotaka bila kutoa hesabu. Mume bahili humkasirisha mkewe na kumfanya kuwa mbadhirifu, kama vile ambavyo mume mbadhirifu au mfujaji anavyomfanya mke kuwa bahili. Kuonyesha imani katika uwezo wa kusimamia pesa kwa mwenzako kwa kawaida kutamfanya apende kuwa makini katika kushugulikia pesa. Kuzungumza mambo pamoja kutaepuka makosa mengi yanayoweza kuharibu ndoa yenu.

**17. Zungumza mambo na kushauriana pamoja kwa uhuru.**

"[Upendo] haukazani kumwonyesha mtu sifa zake, wala hauthamini mawazo ya kuvimba kichwa kwa kujiona muhimu . ... haukasiriki haraka." 1 Wakorintho 13:4 , 5 , Phillips.* "Akataaye mafundisho huidharau nafsi yake mwenyewe." Mithali 15:32 . "Je! waona mtu mwenye hekima machoni pake? Kuna matumaini zaidi ya mpumbavu kuliko yeye." Mithali 26:12 .

**Jibu: K**ushauriana juu ya maamuzi yote makubwa kutasaidia mambo mengi kuliko mengi utayayofanya. Kubadilisha kazi au kununua nyumba, gari, jahazi, samani, mavazi (angalau vitu vikubwa), na vitu vingine vyote vinavyohitaji pesa, mume na mke wote wahusike, na maoni ya wote wawili yanapaswa kuzingatiwa. Kuzungumza mambo pamoja kutaepuka makosa mengi yanayoweza kuharibu ndoa yenu. Ikiwa, baada ya mazungumzo mengi na maombi ya bidii, maoni yenu bado yanatofautiana, mke anapaswa kutii uamuzi wa mume wake. Maandiko yako wazi juu ya hili. (Angalia Waefeso 5:22-24 .)

**18. Nataka nyumba yangu iwe mahali ambapo malaika wa mbinguni hufurahia kutembelea.**

**Jibu:**

## MASWALI YA KUFIKIRIA NA KUCHEUA

**1. Ni mwenzi gani wa ndoa anayepaswa kuwa wa kwanza kuungama baada ya ugomvi?**

Yule ambaye alikuwa sahihi! (Yule ambaye hakukosea)

**2. Je, unaweza kupendekeza sheria kwa mama mkwe msumbufu?** Ndiyo! Kaa kimya na uangalie mambo yako mwenyewe! (Ona 1 Wathesalonike 4:11.) Kwa kweli, sheria hii inatumika kwa wakwe wote. Ndoa nyingi ambazo zinaweza kuwa mbinguni kidogo duniani zimebadilishwa kuwa jehanamu na wakwe. Wajibu wa wakwe wote ni kuacha ndoa mpya au changa peke yake kwanza.

**3. Mume wangu ni mtu asiyemcha Mungu, na ninajaribu kuwa Mkristo. Ushawishi wake ni wa kutisha. Je, nimpe talaka?**

Hapana! Soma 1 Wakorintho 7:12-14 na 1 Petro 3:1 , 2 . Mungu hutoa jibu maalum.

**4. Mume wangu akinichukiza, sitalala naye. Anasema nimekosea. Je! ni mimi?**

Ndiyo! Mungu anatoa jibu la uhakika kwa swali hili katika 1 Wakorintho 7:4 , 5 .

**5. Mke wangu alikimbia na mwanamume mwingine. Sasa akiwa ametubu, anataka kurudi nyumbani. Mchungaji wangu anasema nimrudishe, lakini Mungu anakataza jambo hili, au sivyo?**

Hapana. Hapana! Mungu anaruhusu talaka kwa uzinzi, lakini haamrishi umwache mwenzi au umpe talaka. Msamaha daima ni bora na daima ni njia ya utaratibu wa mbinguni. (Angalia Mathayo 6:14 , 15 .) Talaka itaharibu sana maisha yako na ya watoto wako. Mpe nafasi nyingine! Kanuni ya dhahabu au golden rule (Mathayo 7:12 ) inatumika hapa. Ikiwa wewe na mke wako mtakabidhi maisha yenu kwa Kristo, Yeye ataifanya ndoa yenu kuwa na furaha kuu. Hujachelewa bado.

**6. Ninaweza kufanya nini? Wanaume kila wakati wanajaribu kufahamiana nami kwa ukaribu.**

Kuwa makini sana na mwenendo wako. Mungu anasema, “Jiepusheni na uovu wote.” 1 Wathesalonike 5:22 . Labda mwenendo wako kwa wanaume--tabasamu la linalokaribisha, mavazi yasiyo yasiyo na kujistahi, utani usio na adabu, au mtazamo “wa kujiachia ukiwa na wanaume” na una jinsi ya kuwaalika wakutongoze--na wasonge mbele, kama si wale wanaokushika kwa nguvu, wewe unaweza kujiepusha nao kwa kuwaambia imani yako na jinsi unavyothamini mpango wa ndoa aliotoa Mungu, utashangaa wanakukimbia, hata pale wanapozungumza maneno machafu wataenda mbali kuambiana na watasema yule “fulani” huwa hataki upuuzi huu, wacha twende kwa mdada mwingine au mkaka mwingine. Kuna kitu kuhusu kujistahi kwa Kikristo na kutunza hadhi ambako humweka mtu mahali pake. Kristo alisema, “Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.” Mathayo 5:16 . Kristo anapoangaza kutoka kwa maisha yako, utakuwa na shida pungufu au kidogo na watu waovu na

uchafu wao wa kutongoza wanandoa.

**7. Je, unaweza kuniambia kwa urahisi na kwa uwazi ushauri wa Mungu ni nini kwa mtu ambaye ameanguka lakini ametubu kikweli?**

Zamani sana Kristo alitoa jibu lililo wazi na la kufariji kwa mtu ambaye alikuwa ameanguka katika ukosefu wa maadili lakini akatubu. Yeye "Akasema, Nenda zako, wala usitende dhambi tena". Yohana 8:11 . Shauri Lake bado linatumika leo. Nenda na usitende dhambi tena yaani kama umeshaitenda, usiirudie tena!

**8. Je, "mtu asiye na hatia" katika talaka wakati mwingine anawez akuwa ana hatia pia?**

Hakika. Wakati mwingine "yule asiye na hatia," kwa kutokuwa na upendo, kutojali, kujiona kuwa ni mwadilifu, kutokuwa na fadhili, kuwa na ubinafsi, kumkera na kumsumbua mwenzake, na kuwa na ubaridi au ukavukavu, kunaweza kuhimiza mawazo na matendo mabaya kwamwenzi wake wa ndoa. Wakati mwingine "yule anayeonekana hana hatia" anaweza kuwa na hatia sawa mbele ya Mungu kama "mwenye hatia". Mungu anaangalia nia zetu Naye anahukumu ipasavyo. "Maana Bwana haangalii kama mwanadamu atazamavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo." 1 Samweli 16:7 .

**9. Je, Mungu anatarajia niishi na mwenzi anayeninyanyasa kimwili? (Kunipiga nk)**

Unyanyasaji wa kimwili unaweza kutishia maisha na ni tatizo kubwa linalohitaji uangalizi wa haraka. Mwenzi na wanafamilia ambao wamenyanyaswa kimwili lazima wapate mazingira salama ya kuishi. Mume na mke wahitaji kutafuta msaada wa kitaalamu kupitia mshauri wa ndoa wa Kikristo anayefaa. Watu wengine wameoa au kuolewa na watu ambao ni wakatili au wenye maradhi ya akili 'narcist', jambo hili ni hatarishi, tafuta msaada wa ushauri, na kama ni mtu ambaye anadhuru maisha, inabidi hatua za usalama hata za nchi zichukuliwe mapema, shauriana na watu wa karibu kwa haraka inavyowezekana, ili mwenzi wako pia aweze pia kupata msaada.

# MASWALI YA CHEMSHA BONGO KWIZZ

**1. Ndoa ni (1)**
_____ Kuunganishwa kwa mwanamume na mwanamke pamoja na Mungu kwa maisha yote.
_____ Mkakati wa muda ambao ni majaribio ya kuishi pamoja ili kuona kama mnaweza kukaa kuendana pamoja.
_____ Hata sio lazima. Wanaume na wanawake wako huru kuishi pamoja bila hiyo.

**2. Mungu anatambua sababu moja tu ya talaka. Ni (1)**
_____ Kutopatana.
_____ Mchumba mwenye hasira.
_____ Uzinzi au uasherati.
_____ Kutomcha Mungu kwa mwenzi wa ndoa.

**3. Kujaliana katika uchumba (1)**
_____ Kunapaswa kuendelea katika maisha ya ndoa.
_____ Kunapaswa kuachwa haraka baada ya harusi.
_____ Ni ujinga mtupu na sio lazima.

**4. Dhamana bora ya mafanikio katika ndoa ni (1)**
_____ Kuwa na Kristo moyoni na nyumbani.
_____ Mume kumlazimisha mke wake awe kwenye mstari.
_____ Mke kujifanyia apendavyo kwa kutishia talaka.

**5. Kwa usalama pale kwenye ugomvi, fanya yafuatayo: (3)**
_____ Zungumza kwa upole na fadhila kwa mwenzi wako.
_____ Mfanye mwenzi wako akubali makosa.
_____ Waite majirani kusuluhisha mambo.
_____ Mlazimishe mwenzi wako kunyamaza.
_____ Ondoka ndani ya nyuma na ukae mbali kwa siku kadhaa.
_____ Ombeni pamoja.
_____ Dhibiti hasira yako kabla ya kulala usiku.

**6. Angalia vitu ambavyo ni funguo za mafanikio katika ndoa: (2)**
_____ Funga mzunguko wa familia usingiliwe na watu wengine.
_____ Ishi katika nyumba ya wazazi wako.
_____ Kimbia nyumbani kwa mama ukiwa na hasira.
_____ Waambie marafiki wa karibu makosa ya mwenzi wako.
_____ Anza nyumba yako binafsi mahali pengine.
_____ Mwandikie mpenzi wa zamani kwa ushauri.
_____ Kamwe usikiri kwanza baada ya kutema mate chini.

**7. Njia bora za kuboresha mwenzi wako wa ndoa ni (2)**
_____ Kutishia kuondoka isipokuwa njia yako itathaminiwa.
_____ Mkere mwenzao na kumkosoa.
_____ Boresha uhusiano wako mwenyewe na Yesu Kristo.

_____ Mfanye mwenzako alale peke yake.
_____ Kuwa na upendo, shukrani, na kusamehe.
_____ Mlazimishe mwenzako kubadilika.

**8. Angalia vitu vilivyo hapa chini vinavyohatarisha ndoa: (6)**
_____ Ukosoaji.
_____ Mume bahili au mchoyo.
_____ Mke mbaradhifu wa pesa.
_____ Uvivu.
_____ Nyumba ya Kikristo.
_____ Kuomba pamoja.
_____ Matatizo na uchafu.
_____ Roho ya kusamehe.
_____ Wivu.

**9. Ili kufanikiwa katika kufanya maamuzi makuu, (2)**
_____ Mume na mke wanapaswa kushauriana pamoja.
_____ Mume alazimishe mapenzi yake kwa mke wake.
_____ Mungu atafutwe katika maombi pamoja.
_____ Sisitiza kuwa na njia yako mwenyewe.

**10. Sheria nzuri kwa wakwe ni (1)**
_____ Endelea na shuguli zako na kuwaacha waliooana hivi karibuni kujua jinsi ya kuchukuliana wao kwa wao.
_____ Sisitiza kwamba waliooana hivi karibuni waishi nawe.
_____ Amua kuwashauri waliooana hivi karibuni kama wanataka au la.

**11. Katika kesi ya kutokuwa mwaminifu kwa mwenzi wako, jambo bora zaidi kufanya ni (1)**
_____ Kuondoka mara moja na usirudi tena.
_____ Mara moja mwambie kila mtu jinsi mpenzi wako asivyopenda haki.
_____ Uwe tayari kusamehe na kuhifadhi nyumba yako, kama itawezekana.

**12. Mawazo yanapaswa kulindwa kwa uangalifu kwa sababu (2)**
_____ Mawazo machafu husababisha matendo machafu.
_____ Mwenzi wako anaweza kusoma mawazo yako.
_____ Mawazo mabaya yataharibu ndoa yako.

**Imeandikwa Kwenye Jiwe**

**Somo la 6**

Karne nyingi zilizopita, Mungu aliandika sheria Yake kwenye jiwe, na bado unatakiwa kuitunza leo! Ni kweli kabisa kwamba kukiuka sehemu yoyote ya sheria ya Mungu daima huleta matokeo mabaya. Uhalifu unapotawala miji yetu, je, haileti vichwani mwetu dhana kwamba ili kuwa na amani na usalama tunapaswa kuitii sheria za nchi? Naam, kanuni hii inatumika na sheria ya Mungu pia - Amri Kumi - katika maisha yetu wenyewe! Hizi haziitwi mapendekezo kumi, mashauri kumi, au mawazo kumi makuu. Kwa kuwa mengi yako hatarini, unapaswa kuchukua dakika chache kufikiria kwa uzito wajibu wako.

Na hizoMbao mbili za Mawe zilikuwa kazi ya Mungu.

**1. Je, ni kweli Mungu Mwenyewe Ndiye aliyeandika Amri Kumi?**
"Kisha akampa Musa ... mbao mbili za ushuhuda, mbao za mawe, zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu." "Na zile mbao zilikuwa kazi ya Mungu, na maandishi hayo yalikuwa maandishi ya Mungu, yaliyoandikwa katika hizo mbao." Kutoka 31:18 ; 32:16 .

**Jibu:** Ndiyo, Mungu mkuu wa mbinguni aliandika Amri Kumi kwenye mbao za mawe kwa kidole Chake Mwenyewe.

Mungu anasema kwamba dhambi ni kuvunja sheria Yake.

**2. Je, ufafanuzi wa Mungu wa dhambi ni upi?**
"Dhambi ni uvunjaji wa sheria." 1 Yohana 3:4 .

**Jibu:** Dhambi ni kuvunja sheria ya Amri Kumi za Mungu. Na kwa kuwa sheria ya Mungu ni kamilifu ( Zaburi 19:7 ), inafunika kila dhambi inayoweza kufikiriwa. Haiwezekani kutenda dhambi ambayo haijashutumiwa na angalau ile moja ya Amri Kumi za Mungu. Amri zinafunika "wajibu wote wa mwanadamu." Mhubiri 12:13 . Hakuna kinachoachwa.

Furaha hufuata wale wanaozishika amri Zake.

**3. Kwa nini Mungu alitupa Amri Kumi?**
"Heri yeye aishikaye sheria." Mithali 29:18. "Zishike amri Zangu; Maana zitakuongezea wingi wa siku, na maisha marefu, na amani." Methali 3:1 , 2 .

**Jibu:**
A. Ili uwe mwongozo wa maisha yenye furaha na uzima tele.
Mungu alituumba ili tufurahi, tuwe na amani, maisha marefu, kuridhika, kuweza kutimiza mambo fulani, na baraka nyingine zote kuu ambazo mioyo yetu inatamani kupata. Sheria ya Mungu ndiyo ramani inayoonyesha njia zinazofaa za kufuata ili kupata furaha hii ya Kweli na kuu.

“Kujua dhambi ni kwa sheria.” Warumi 3:20 . “Singalijua dhambi, bali kwa sheria; Warumi 7:7 .

B. Ili kunionyesha tofauti kati ya mema na mabaya.
Sheria ya Mungu ni kama kioo ( Yakobo 1:23-25 ). Inaonyesha makosa katika maisha yangu kama kioo kinavyoonyesha uchafu usoni mwangu. Njia pekee inayowezekana ya mtu kujua ikiwa anatenda dhambi ni kuchunguza maisha yake kwa uangalifu kwa kioo cha sheria ya Mungu. Tumaini kwa kizazi hiki kilichochanganyika na kuzama Linapatikana katika sheria ya Amri Kumi za Mungu. Inatueleza wapi tunapaswa kupiga mstari wa mpaka!

“Na Bwana akatuamuru kuzifanya amri [amri] hizi zote ... kwa faida yetu siku zote.” Kumbukumbu la Torati 6:24 . “Unishike nami nitakuwa salama, nami nitaziangalia amri Zako daima. Umewakanyaga wote wazikosao amri Zako.” Zaburi 119:117 , 118 .

C. Ili kunilinda na hatari na majanga.
Sheria ya Mungu ni kama ngome yenye nguvu kwenye bustani ya wanyama, ambayo hutulinda dhidi ya wanyama wakali na waharibifu. Inatulinda dhidi ya uchafu, uwongo, mauaji, ibada ya sanamu, wizi, na maovu mengine mengi ambayo huharibu maisha, amani, na furaha. Sheria zote nzuri hulinda, na sheria ya Mungu ndivyo ilivyo.

**Angalizo Maalum:** Kanuni za milele za sheria ya Mungu zimeandikwa ndani kabisa ya asili ya kila mtu na Mungu aliyetuumba. Maandishi yanaweza kuwa hafifu na kuchafuka, lakini bado yapo. Hili lamaanisha, bila shaka, kwamba huwezi kupata amani ya kweli isipokuwa uwe tayari kuishi kupatana na asili yako ya ndani, ambayo kwayo Mungu ameandika kanuni hizi. Tuliumbwa kuishi kwa kupatana na sheria ya Mungu. Tunapochagua kuzipuuza, matokeo yake huwa ni mvutano, machafuko na misiba, kama vile kupuuza sheria za uendeshaji salama husababisha matatizo makubwa.

Sheria inatulinda na shetani kama ngome inavyotulinda na simba kwenye mbuga ya wanyama.

**4. Kwa nini sheria ya Mungu ni muhimu sana kwangu binafsi?**
“Neneni na kufanya hivyo kama wale watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru.” Yakobo 2:12 .

**Jibu:** Kwa sababu sheria ya Amri Kumi ni kiwango ambacho Mungu huwachunguza watu katika hukumu ya mbinguni. Je, wewe unaijali sheria? Ni suala la maisha au kifo!
Msalaba ni uthibitisho chanya kwamba sheria haiwezi kubadilika.

**5. Je, sheria ya Mungu (Amri Kumi) inaweza kubadilishwa au kukomeshwa?**
“Ni vyepesi zaidi mbingu na nchi vitoweke, kuliko kutotimia kwa nukta moja ya torati.” Luka 16:17. “Sitalivunja agano Langu, wala sitalibadili Neno lililotoka midomoni Mwangu.” Zaburi 89:34 . “Amri Zake zote ni amini, zimesimama imara milele na milele.” Zaburi 111:7 , 8 .

**Jibu:** Hapana kabisa! Biblia iko wazi sana kuhusu jambo hili. Ikiwa sheria ingebadilishwa, Mungu angefanya badiliko hilo mara moja Adamu na Hawa walipofanya dhambi badala ya kumtuma Mwana Wake afe kwa ajili ya mtenda-dhambi ili kulipa adhabu ya sheria iliyovunjwa. Lakini hii haikuwezekana, kwa sababu amri sio sheria kwa maana ya kanuni au mswada ambao umetungwa katika bunge. Ni kanuni zilizofichuliwa za tabia takatifu ya Mungu ambazo zitakuwa Kweli siku zote maadamu Mungu Yupo.

Angalia kwenye chati iliyo hapa chini kwamba Mungu na sheria Yake wana sifa sawa. Unaona hii inamaanisha nini? Sheria ya Amri Kumi ni tabia ya Mungu iliyoandikwa ili tuweze kuielewa. Haiwezekani kubadili sheria ya Mungu kama vile ambavyo haiwezekani kumtoa Mungu kutoka mbinguni na kumbadilisha. Yesu alikuja kutuonyesha jinsi sheria (ambayo ni kielelezo cha maisha matakatifu) ilionekana ilipoundwa katika umbo la mwanadamu. Tabia ya Mungu haiwezi kubadilika kamwe. Wala sheria Yake haiwezi, kwa kuwa ni tabia Yake katika lugha ya kibinadamu.

| | **MUNGU NI** | **SHERIA NI** |
|---|---|---|
| Nzuri | Luka 18:19 | 1 Timotheo 1:8 |
| Mtakatifu | Isaya 5:16 | Warumi 7:12 |
| Kamilifu | Mathayo 5:48 | Zaburi 19:7 |
| Safi | 1 Yohana 3:2 , 3 | Zaburi 19:8 |
| Sahihi | Kumbukumbu la Torati 32:4 | Warumi 7:12 |
| Ya Kweli | Yohana 3:33 | Zaburi 19:9 |
| Kiroho | 1 Wakorintho 10:4 | Warumi 7:14 |
| Ya Haki | Yeremia 23:6 | Zaburi 119:172 |
| Aminifu | 1 Wakorintho 1:9 | Zaburi 119:86 |
| Upendo | 1 Yohana 4:8 | Warumi 13:10 |
| Haibadiliki | Yakobo 1:17 | Mathayo 5:18 |
| Milele | Mwanzo 21:33 | Zaburi 111:7 , 8 |

Yesu ni sheria katika umbo la mwanadamu. Yeye Anapokuwa moyoni, kuishika sheria huwa raha.

**6. Je, Yesu alibatilisha sheria ya Mungu alipokuwa hapa duniani?**
"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati.... sikuja kutangua, bali kutimiliza.... Mpaka mbingu na nchi zitakapopita, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie." Mathayo 5:17 , 18 .
Jibu: Hapana, kwa kweli Yesu alisisitiza hasa kwamba hakuja kuiharibu sheria, bali

kuitimiza (au kushika). Badala ya kuiondoa sheria, Yesu aliitukuza ( Isaya 42:21 ) kama mwongozo kamili wa kuishi kwa haki. Kwa mfano, Yesu alionyesha kwamba "usiue" hushutumu kuwa na hasira "bila sababu" ( Mathayo 5:21 , 22 ) na chuki ( 1 Yohana 3:15 ), na kwamba tamaa ni uzinzi ( Mathayo 5:27 , 28 ) ) Anasema, "Mkinipenda, mtazishika amri Zangu." Yohana 14:15 .
Sheria ni kama urefu wa mnyororo. Ikiwa kiungo kimoja tu kimevunjwa, madhumuni yake yote yameharibiwa.

**7. Je, watu ambao kwa kujua wataendelea kuvunja hata amri moja ya Mungu wataokolewa?**
"Mshahara wa dhambi ni mauti." Warumi 6:23 . "Atawaangamiza wenye dhambi." Isaya 13:9 . "Yeyote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika Neno moja, amekosa juu ya yote." Yakobo 2:10 .

**Jibu:** Hapana! Watapotea. Sheria ya Amri Kumi ndiyo mwongozo tunaopaswa kuutumia katika kutafuta njia yetu kwa Mungu na maisha matakatifu. Nikipuuza hata amri moja, ninapuuza sehemu ya muundo wa Bwana, au ramani. Ikiwa kiungo kimoja tu cha mnyororo kitavunjwa, madhumuni yake yote yatabatilishwa. Biblia inasema kwamba tunapovunja amri yoyote ya Mungu kwa kujua, tunafanya dhambi ( Yakobo 4:17 ), kwa sababu tumekataa mapenzi Yake kwetu. Ni wale tu wanaofanya mapenzi Yake ndiyo wanaweza kuingia katika ufalme wa mbinguni. Wenye dhambi watapotea.
Wokovu kutoka kwa Yesu ni halisi sawa na zawadi iliyopokelewa kwenye sikukuu maalum au siku ya kuzaliwa. Ni bure, na umetayarishwa mahususi kwa ajili yetu kutoka kwa Yesu!

**8. Je, mtu yeyote anaweza kuokolewa kwa kushika sheria?**
"Kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele Zake." Warumi 3:20 . "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu." Waefeso 2:8 , 9 .

**Jibu:** Hapana! Jibu ni rahisi sana kukosea. Hakuna anayeweza kuokolewa kwa kushika sheria. Wokovu huja tu kupitia neema, kama zawadi ya bure kutoka kwa Yesu Kristo, na tunapokea zawadi hii kwa imani, si kwa matendo. Sheria hutumika tu kama kioo cha kuonyesha dhambi katika maisha yetu. Utakaso na msamaha kutoka kwa dhambi hiyo huja kupitia Kristo pekee. Ukijitazama kwenye kioo ukakuta meno yako yana mboga au maharage uliyokula, je kioo kitasaidia kutoa haya maharage au mboga kwenye meno?
Viwango vyetu wenyewe si salama kamwe. Siwezi kujua kama mimi ni mwenye dhambi isipokuwa niangalie kwa makini kiwango kikamilifu, yaani kioo cha sheria cha Mungu.

**9. Kwa nini, basi, sheria ni muhimu kabisa kwa ajili ya kukamilisha tabia ya Kikristo?**
"Mche Mungu, nawe uzishike amri Zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu." Mhubiri 12:13. "Kujua dhambi ni kwa sheria." Warumi 3:20 .

**Jibu:** Kwa sababu muundo kamili, au "wajibu mzima," kwa maisha ya Kikristo yamo katika sheria ya Mungu. Kama mvulana wa miaka 6 aliyejitengenezea mtawala, akajipima, na kumwambia mama yake kwamba alikuwa na urefu wa futi 12, viwango vyetu si salama kamwe. Siwezi kujua kama mimi ni mwenye dhambi isipokuwa niangalie kwa makini kiwango kamilifu, kioo cha sheria cha Mungu. Mamilioni ya watu ambao wametoa pepo, kutabiri, na kufanya kazi nyingi za ajabu katika Jina la Yesu watapotea ( Mathayo 7:21-23 ) kwa sababu hawakujisumbua kuchunguza maisha yao kwa kielelezo Chake kikuu cha sheria. Kwa hiyo, wanafikiri wao ni wenye haki na kuokolewa wakati, badala yake, wao ni wenye dhambi na wamepotea. "Katika hili twajua ya kuwa tumemjua Yeye, ikiwa tunashika amri Zake." 1 Yohana 2:3 .

Yesu akiishi moyoni, maisha ya giza na mabaya yanabadilishwa na kuishi kwake kwa ushindi.

**10. Ni nini humwezesha Mkristo aliyeongoka kikweli kufuata kielelezo cha sheria ya Mungu?**

"Nitatia sheria Zangu katika nia zao, na katika mioyo yao nitaziandika." Waebrania 8:10 . "Nayaweza mambo yote katika Kristo." Wafilipi 4:13 . "Mungu akimtuma Mwanawe Mwenyewe ... Ili haki ya torati itimizwe ndani yetu." Waroma 8:3 , 4 .

**Jibu:** Kristo hawasamehe tu wenye dhambi wanaotubu, bali anarudisha ndani yao sura ya Mungu. Yeye Anawaleta katika upatanifu na sheria Yake kupitia kwa uwezo wa uwepo Wake ndani yake. Katazo la "Usifanye" basi linakuwa ahadi kwamba Mkristo hataiba, hatasema uongo, au kuua, nk, kwa sababu Yesu anaishi ndani na anatawala. Mungu hangeweza kubadili sheria Yake, lakini alifanya mpango uliobarikiwa kupitia Yesu ili kumbadilisha mwenye dhambi ili aweze kufikia sheria hiyo.

Msamaha wa Rais husamehe mfungwa, lakini haumpi uhuru wa kuvunja sheria moja.

**11. Lakini je, Mkristo aliye na imani na anayeishi chini ya neema, si amefunguliwa kutoka kwa kushika sheria?**

"Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa maana hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema. Je! tutende dhambi [tunavunja sheria] kwa sababu hatuko chini ya sheria, bali chini ya neema? Hasha! Waroma 6:14 , 15 . "Basi, je! twaibatilisha sheria kwa imani? Hasha; naam, twaithibitisha sheria." Warumi 3:31 .

**Jibu:** Hapana! Maandiko yanafundisha kinyume kabisa. Neema ni kama msamaha wa Rais kwa mfungwa. Inamsamehe, lakini haimpi uhuru wa kuvunja hata sheria moja kwenye vitabu vya sheria. Mtu aliyesamehewa, na anayeishi chini ya neema, yuko chini ya wajibu maradufu wa kushika sheria. Mtu anayekataa kushika sheria ya Mungu, akisema kwamba anaishi chini ya neema, amekosea. Anaishi chini ya fedheha.

**12. Je, Amri Kumi za Mungu zimethibitishwa tena katika Agano Jipya?**

**Jibu:** Ndiyo, na kwa uwazi kabisa hivyo. Angalia yafuatayo kwa makini sana.

| SHERIA YA MUNGU KATIKA AGANO JIPYA | SHERIA YA MUNGU KATIKA AGANO LA KALE |
|---|---|
| 1. “Utamwabudu Bwana, Mungu wako, umwabudu Yeye peke yake.” Mathayo 4:10 . | 1. “Usiwe na miungu mingine ila Mimi.” Kutoka 20:3 . |
| 2. “Watoto wadogo, jilindeni na sanamu.” 1 Yohana 5:21 . “Basi, kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu, haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa dhahabu au fedha au jiwe, vilivyochongwa kwa ustadi na akili ya mwanadamu.” Matendo 17:29 . | 2. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia; usisujudie. wala kuwatumikia; kwa kuwa Mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao; nawarehemu maelfu elfu wanipendao na kunishika. amri Zangu.” Kutoka 20:4-6 . |
| 3. “Ili Jina la Mungu na mafundisho Yake yasitukanwe.” 1 Timotheo 6:1 . | 3. “Usilitaje bure Jina la Bwana, Mungu wako, kwa kuwa Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye Jina lake bure.” Kutoka 20:7 . |
| 4. “Maana aliinena siku ya saba mahali fulani hivi, Mungu alistarehe siku ya saba, akaziacha kazi Zake zote. “Basi, imesalia raha [“kuitunza Sabato,” kando] kwa watu wa Mungu. Waebrania 4:4 , 9 , 10 . | 4. “Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, fanya mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako; siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe wala. mwana wako, wala binti yako, mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala ng’ombe wako, wala mgeni aliye ndani ya malango yako; siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya sabato akaitakasa.” Kutoka 20:8-11 . |
| 5. “Waheshimu baba yako na mama yako.” Mathayo 19:19 . | 5. “Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako.” Kutoka 20:12 . |
| 6. “Usiue.” Warumi 13:9 . | 6. “Usiue.” Kutoka 20:13 . |
| 7. “Usizini.” Mathayo 19:18 . | 7. “Usizini.” Kutoka 20:14 . |
| 8. “Usiibe.” Warumi 13:9 . | 8. “Usiibe.” Kutoka 20:15 . |
| 9. “Usishuhudie uongo.” Warumi 13:9 . | 9. “Usitoe ushahidi wa uongo dhidi ya jirani yako.” Kutoka 20:16 . |
| 10. “Usitamani.” Warumi 7:7 . | 10. “Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako, wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng’ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako.” Kutoka 20:17 . |

Dhabihu za maadhimisho/sherehe na desturi zilielekeza mbele kwenye dhabihu ya Yesu.

**13. Je! Sheria ya Mungu na sheria ya Musa ni sawa?**
**Jibu:** Hapana, hazifanani. Jifunze maelezo yafuatayo na ulinganishe kwa makini.

Kumbuka: Sheria ya Musa ilikuwa sheria ya muda, ya maadhimisho/sherehe ya Agano la Kale. Ilidhibiti ukuhani, dhabihu, matambiko, sadaka za nyama na vinywaji, n.k., vyote hivyo vilikuwa kivuli cha msalaba. Sheria hii iliongezwa "mpaka uzao au mbegu ya mwanamke atakapokuja," na uzao huo ulikuwa Kristo ( Wagalatia 3:16 , 19 ). Tambiko na sherehe za sheria ya Musa zilielekeza mbele kwenye dhabihu ya Kristo. Alipokufa, sheria hii ilifikia mwisho, lakini Amri Kumi (sheria ya Mungu) " Zimesimama milele na milele." Zaburi 111:8 . Kwamba kuna sheria mbili imewekwa wazi kabisa katika Danieli 9:10 , 11 .

**Angalizo Maalum:** Tafadhali kumbuka kwamba sheria ya Mungu imekuwepo angalau kwa muda mrefu pengine hata kabla ya dhambi kuwepo au ……. Biblia inasema, "Pasipo sheria, hakuna kosa [au dhambi]." Warumi 4:15 . Kwa hiyo sheria ya Amri Kumi za Mungu ilikuwepo tangu mwanzo. Wanadamu walivunja sheria hiyo (walifanya dhambi, 1 Yohana 3:4 ). Kwa sababu ya dhambi (au kuvunja sheria ya Mungu), sheria ya Musa ilitolewa (au "iliongezwa" Wagalatia 3:16 , 19 ) mpaka Kristo aje na kufa. Sheria mbili tofauti zinahusika: Sheria ya Mungu na Sheria ya Musa.

| SHERIA YA MUSA | SHERIA YA MUNGU |
|---|---|
| Inaitwa "sheria ya Musa" ( Luka 2:22). | Inaitwa "sheria ya Bwana" ( Isaya 5:24) |
| Inaitwa "sheria ... iliyo ndani ya maagizo" (Waefeso 2:15 ). | Inaitwa "sheria ya kifalme" (Yakobo 2:8 ). |
| Imeandikwa na Musa katika kitabu (Mambo ya Nyakati 35:12 ). | Imeandikwa na Mungu kwenye jiwe ( Kutoka 31:18). 32:16 ). |
| Imewekwa ubavuni mwa safin (Kumbukumbu la Torati 31:26 ). | Kuwekwa ndani ya safina (Kutoka 40:20 ). |
| Iliishia msalabani ( Waefeso 2:15 ). | Atasimama milele ( Luka 16:17 ). |
| Imeongezwa kwa sababu ya dhambi (Wagalatia 3:19 ). | Anaonyesha dhambi (Warumi 7:7). 3:20 ). |
| Kinyume na sisi, dhidi yetu (Wakolosai 2:14 ). | Sio huzuni ( 1 Yohana 5:3 ). |
| Hawahukumu mtu yeyote (Wakolosai 2:14-16 ). | Huhukumu watu wote ( Yakobo 2:10-12). |
| Kimwili ( Waebrania 7:16 ). | Kiroho ( Warumi 7:14 ). |
| Hakukamilisha chochote ( Waebrania 7:19 ). | Mkamilifu ( Zaburi 19:7 ). |

Joka akamkasirikia yule mwanamke [kanisa la kweli].

**14. Ibilisi anahisije kuhusu watu wanaofuata amri kumi za Mungu maishani mwao?**
"Joka [Ibilisi] akamkasirikia yule mwanamke [kanisa la Kweli], akaenda zake afanye vita juu ya wazao Wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu." Ufunuo 12:17 . "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu." Ufunuo 14:12 .

**Jibu:** Ibilisi anachukia watu wanaoshika sheria ya Mungu kwa sababu sheria ni kielelezo cha maisha ya haki. Na ukiamua kufuata utaratibu ulioainishwa katika sheria ya Mungu, utasikia ghadhabu ya shetani juu yako mara moja na kwa ghadhabu yote. Haishangazi kwamba shetani anachukia na kuwapinga vikali wote wanaoshika sheria ya Mungu. Lakini inashangaza na kustaajabisha kuwasikia viongozi wa kidini wakikana madai ya lazima ya Amri Kumi na wakati huo huo wakishikilia mapokeo ya wanadamu. Si ajabu Yesu alisema, "Mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu? "Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu." Mathayo 15:3 , 9 .

Naye Daudi akasema, "Ni wakati wa Wewe, Bwana, kufanya kazi, kwa maana wameibatilisha sheria Yako." Zaburi 119:126 . Wakristo wanapaswa kuamka na kuirejesha sheria ya Mungu kwenye nafasi yake ya haki, iliyotukuka. Ni upumbavu kwa kizazi hiki kisicho na nidhamu kudhani kwamba kinaweza kuvunja sheria za Mungu aliye hai bila kuadhibiwa.

**15. Ninaamini Mkristo lazima azitii Amri Kumi za Mungu, na ninamwomba Yesu anisaidie kuleta maisha yangu katika upatano nazo.**

**Jibu:**
**Maswali ya Kutafakari na Kucheua**
**1. Je, Biblia haisemi sheria ilikuwa (au) ina kasoro?**

Hapana. Biblia inasema watu hao walikuwa na makosa. Mungu alipata "kosa kwao." Waebrania 8:8 . Na katika Warumi 8:3 Biblia inasema kwamba torati "ilikuwa dhaifu kwa sababu ya mwili." Daima ni kisa sawa. Sheria ni kamilifu, lakini watu wana makosa, au ni dhaifu. Kwa hiyo Mungu angetaka Mwanawe aishi ndani ya watu Wake "ili haki ya torati itimizwe ndani yetu" ( Warumi 8:4 ) kupitia Kristo anayekaa ndani Yake.

**2. Wagalatia 3:13 inasema tumekombolewa kutoka katika laana ya sheria. Je, unaweza kueleza hili?**
Laana ya sheria ni mauti ( Warumi 6:23 ). Kristo alionja "mauti kwa ajili ya kila mtu." Waebrania 2:9 . Hivyo aliwakomboa wote kutoka katika laana ya sheria (kifo) na mahali pake akatoa uzima wa milele

**3. Je, Wakolosai 2:14-17 na Waefeso 2:15 haifundishi kwamba sheria ya Mungu iliishia msalabani?**

Hapana, vifungu hivi vyote viwili vinarejelea sheria iliyo na "maagizo," au sheria ya Musa, ambayo ilikuwa sheria ya sherehe inayoongoza mfumo wa dhabihu na ukuhani. Sherehe hizi zote na tambiko zilionyesha huko mbeleni, yaani zilikuwa kivuli cha msalaba na kuishia katika kifo cha Kristo, kama Mungu alivyokusudia. Sheria ya Musa iliongezwa mpaka "Mzao atakapokuja," na "uzao huo… Wagalatia 3:19 , 16 . Sheria ya Mungu isingeweza kuhusika hapa, kwa kuwa Paulo aliizungumzia kuwa takatifu, ya haki, na nzuri miaka mingi baada ya msalaba ( Warumi 7:7 , 12 ).

**4. Biblia inasema, "Upendo ni utimilifu wa sheria." Warumi 13:10. Biblia pia, katika Mathayo 22:37-40, inatuamuru kumpenda Mungu na kuwapenda jirani zetu, na inamalizia kwa maneno haya, "Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii." Je, amri hizi huchukua nafasi ya Amri Kumi?**

Hapana, Amri Kumi hutegemea amri hizi mbili kama vile vidole 10 vinavyoning'inia kutoka kwa mikono yetu miwili. Haviwezi kutenganishwa. Kumpenda Mungu hufanya kuzishika amri nne za kwanza (zinazohusu Mungu) kuwa raha, na upendo kwa jirani hufanya kutunza zile sita za mwisho (zinazohusu jirani zetu) kuwa shangwe. Upendo hutimiza sheria kwa kuondoa uchokozi na kwa kuifanya sheria kuwa furaha ( Zaburi 40:8 ). Tunapompenda mtu kikweli, kile anachotuuliza huwa furaha kwetu. Yesu alisema, "Mkinipenda, mtazishika amri Zangu." Yohana 14:15 . Haiwezekani kumpenda Bwana na kutoshika amri Zake, kwa sababu Biblia inasema, "Huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri Zake; na amri Zake si nzito." 1 Yohana 5:3 . "Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake." 1 Yohana 2:4 .

**5. Je, 2 Wakorintho 3:7 haifundishi kwamba sheria iliyoandikwa na kuchongwa kwenye mawe "ilipaswa kuondolewa"?**

Hapana. Fungu linasema kwamba "utukufu" wa huduma ya Musa ya sheria ulipaswa kuondolewa, lakini si sheria. Soma kifungu kizima cha 2 Wakorintho 3:3-9 tena, kwa makini. Somo sio kuondoa sheria au kuanzishwa kwake, lakini badala yake, mabadiliko ya mahali pa sheria kutoka "mbao za mawe" hadi "mbao za moyo." Chini ya huduma ya Musa sheria ilikuwa juu ya mawe. Chini ya huduma ya Roho Mtakatifu, kupitia Kristo, sheria imeandikwa moyoni (Waebrania 8:10 ). Sheria iliyowekwa kwenye ubao wa matangazo ya shule huwa na ufanisi pale tu inapoingia kwenye moyo wa mwanafunzi. Utumishi wa Kristo wa sheria ni mzuri kwa sababu Yeye huhamisha sheria kwenye moyo wa Mkristo. Kisha kushika sheria kunakuwa njia ya kufurahisha na yenye shangwe ya kuishi kwa sababu Mkristo ana upendo wa Kweli kwa Mungu na wanadamu pia.

**6. Warumi 10:4 inasema kwamba "Kristo ni mwisho wa sheria." Kwa hivyo imeisha, sivyo?**

"Mwisho" katika mstari huu unamaanisha kusudi au kitu, kama inavyofanya katika Yakobo 5:11 . Maana ni wazi. Kuwaongoza watu kwa Kristo—ambapo wanapata haki—ndilo lengo, kusudi, au mwisho wa sheria.

**7. Kwa nini watu wengi hukana madai ya lazima ya sheria ya Mungu?**

"Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Basi wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu. Lakini ninyi hamwufuati mwili, bali katika Roho , ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu." Warumi 8:7-9 .

**8. Je, watu wenye haki wa Agano la Kale waliokolewa na sheria?**

Hakuna aliyewahi kuokolewa na sheria. Wote ambao wameokolewa katika nyakati zote wameokolewa kwa neema. Hii "neema ... tulipewa katika Kristo Yesu kabla ya ulimwengu kuwako." 2 Timotheo 1:9 . Sheria inaonyesha tu dhambi. Kristo pekee Ndiye anayeweza kuokoa. Nuhu "alipata neema" ( Mwanzo 6:8 ); Musa alipata neema ( Kutoka 33:17 ); Waisraeli jangwani walipata neema ( Yeremia 31:2 ); na Habili, Henoko, Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Yusufu, na wengine wengi waliostahili katika Agano la Kale waliokolewa "kwa imani" kulingana na Waebrania 11. Waliokolewa kwa kutazamia msalaba; sisi, kwa kuangalia nyuma yake. Sheria ni muhimu kwa sababu, kama kioo, inafichua "uchafu" katika maisha yetu. Bila hivyo, watu ni wenye dhambi lakini hawajui. Hata hivyo, sheria haina uwezo wa kuokoa. Inaweza tu kuonyesha dhambi. Yesu, na Yeye pekee, Ndiye anaweza kumwokoa mtu kutoka katika dhambi. Hii imekuwa Kweli kila wakati, hata katika nyakati za Agano la Kale. ( Matendo 4:10 , 12 ; 2 Timotheo 1:9 ).

**9. Kwa nini wasiwasi kuhusu sheria? Je, dhamiri si mwongozo salama?**

Hapana! Mara elfu, hapana! Biblia inazungumza juu ya dhamiri mbaya, dhamiri iliyochafuliwa, na dhamiri iliyochomwa moto - ambayo hakuna iliyo salama. "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti." Mithali 14:12 . Mungu anasema, "Anayeutumainia moyo wake ni mpumbavu." Mithali 28:26 .

# MASWALI YA CHEMSHA BONGO, KWIZZ

**1. Amri Kumi ziliandikwa na (1)**
_____ Mungu.
_____ Musa.
_____ Mtu asiyejulikana.

**2. Kulingana na Biblia, dhambi ni (1)**
_____ Upungufu wa utu.
_____ Kuvunja sheria ya Mungu.
_____ Chochote kinachoonekana si sawa.

**3. Angalia kauli zinazosema Ukweli kuhusu sheria ya Mungu: (4)**
_____ Ni mwongozo kamili wa maisha ya furaha.
_____ Ni Kama kioo, huonyesha dhambi.
_____ Inalemea na inakandamiza.
_____ Inaweza kunilinda na uovu.
_____ Ina sifa sawa na za Mungu.
_____ Ilighairiwa katika Agano Jipya.
_____ Ni laana.

**4. Sheria ya Amri Kumi za Mungu (1)**
_____ Ilikuwa kwa ajili ya nyakati za Agano la Kale pekee.
_____ Ilikomeshwa na Yesu msalabani.
_____ Haibadiliki kabisa.

**5. Katika siku ya hukumu nitaokolewa ikiwa (1)**
_____ Ninadumisha kumbukumbu bora ya matendo mema.
_____ Ninampenda Bwana, bila kujali kama ninatii Amri Kumi au la.
_____ Uhusiano wangu wa kibinafsi wa upendo na Yesu unaniongoza kutii amri Zake zote.

**6. Watu wanaokolewa kwa (1)**
_____ Kushika sheria.
_____ Kuvunja sheria.
_____ Yesu Kristo peke yake.

**7. Wakristo walioongoka kweli kweli (1)**
_____ Hushika sheria ya Mungu kupitia nguvu za Kristo.
_____ Hupuuza sheria kwa sababu imeondolewa.
_____ Huzingatia kushika amri kuwa sio lazima.

**8. Mtu anayeishi chini ya neema (1)**
_____ Anaweza kuvunja Amri Kumi bila kutenda dhambi.
_____ Amewekwa huru kutoka kwa kushika sheria.
_____ Atashika amri za Mungu kwa furaha.

**9. Upendo hutimiza sheria kwa sababu (1)**
_____ Upendo hubatilisha sheria.
_____ Upendo wa kweli kwa Mungu na mwanadamu hufanya kushika sheria kuwa raha.
_____ Upendo ni muhimu zaidi kuliko utii.

**10. Sheria ya Musa ni (1)**
_____ Kitu sawa na sheria ya Mungu.
_____ Sheria ya sherehe na dhabihu, ambayo ilielekeza mbele kwa Kristo na kuishia msalabani.
_____ Bado inatumika leo.

**11. Watu wanaotii Amri Kumi (1)**
_____ Wote ni Shupavu wa Sheria.
_____ Watapingwa vikali na shetani, anayemchukia Mungu na sheria Yake.
_____ Wanaokolewa kwa kushika sheria.

**12. Angalia taarifa ambazo ni za kweli kuhusu Kristo na sheria: (4)**
_____ Yesu alivunja sheria.
_____ Yesu Ndiye kielelezo kamili cha kibinadamu cha kushika sheria.
_____ Yesu aliifuta sheria.
_____ Yesu alisema, "Mkinipenda, mtazishika amri Zangu."
_____ Yesu aliikuza sheria na alionyesha kwamba inafunika dhambi zote.
_____ Yesu alisema kwamba sheria haiwezi kubadilishwa.

**Siku Iliyopotea katika Historia**

**Somo la** 7

Je, unajua kuna siku muhimu sana ambayo karibu kila mtu ameisahau? Inashangaza kwamba ni watu wachache tu wanaoifahamu, kwa sababu ni moja ya siku muhimu zaidi katika historia yote ya mwanadamu! Sio tu siku ya zamani, lakini ya sasa na ya baadaye. Zaidi ya hayo, kile kilichotokea siku hii iliyopuuzwa kinaweza kuwa na athari kubwa katika maisha yako. Je, ungependa kujua mambo ya ajabu zaidi kuhusu siku hii iliyopotea ya historia? Kisha soma Mwongozo huu wa Utafiti kwa makini.

Yesu alipokuwa hapa duniani, aliabudu siku ya Sabato.

**1. Yesu aliabudu siku gani kwa desturi?**

“Akafika Nazareti, hapo alipolelewa; na kama ilivyokuwa desturi Yake, akaingia katika sinagogi siku ya Sabato, akasimama ili asome.” Luka 4:16 .

**Jibu:** Desturi ya Yesu ilikuwa kuabudu siku ya Sabato.

Siku ya saba ya juma (Jumamosi) ni Sabato.

**2. Lakini ni siku gani ya juma ambayo ni Sabato?**

“Siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako.” Kutoka 20:10 . “Hata Sabato ilipokwisha, ... asubuhi na mapema siku ya kwanza ya juma, walikwenda kaburini. Marko 16:1 , 2 .

**Jibu:** Sabato sio siku ya kwanza ya juma (Jumapili), kama wengi wanavyoamini, lakini siku ya saba (Jumamosi). Angalia kutoka katika Maandiko hayo hapo juu kwamba Sabato ni siku inayokuja kabla tu ya siku ya kwanza ya juma.

Mungu aliifanya Sabato wakati wa Uumbaji.

**3. Ni nani aliyeifanya Sabato na lini?**

“Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.” “Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi Yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi Yake yote aliyoifanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa.” Mwanzo 1:1 ; 2:2 , 3 .

**Jibu:** Mungu aliifanya Sabato wakati wa Uumbaji, alipoumba ulimwengu. Alipumzika siku ya Sabato na kuibariki na kuitakasa (aliitenga kwa matumizi matakatifu).

Mungu aliandika amri ya Sabato kwa kidole Chake Mwenyewe.

**4. Je, Mungu anasema nini kuhusu kushika Sabato katika Amri Kumi, alizoziandika kwa kidole Chake Mwenyewe?**

“Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako; siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe wala mwana wako. wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufugwa, wala mgeni aliye ndani ya malango yako; maana kwa siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi, na bahari na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba. siku; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.” Kutoka 20:8-11 . “Bwana akanipa mbao mbili za mawe zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu.” Kumbukumbu la Torati 9:10 .

**Jibu:** Katika amri ya nne ya zile kumi, Mungu anatuamuru kushika Sabato ya siku ya saba kama siku Yake takatifu. Mungu alijua watu wangesahau Sabato Yake, kwa hiyo alianza amri hii kwa neno “kumbuka”. Hajawahi kuamuru mtu yeyote mahali popote kuweka siku nyingine yoyote kama siku takatifu ya kila juma.

Yesu anasema ni rahisi zaidi mbinguni kupita kuliko sheria ya Mungu kubadilika.

**5. Lakini je, Amri Kumi hazijabadilishwa?**

Yesu anasema: “Na ni vyepesi zaidi mbingu na dunia kupita, kuliko kutimia nukta moja ya torati.” Luka 16:17 . Mungu anasema: “Agano Langu sitalivunja, wala sitalibadili Neno lililotoka midomoni Mwangu.” Zaburi 89:34 . Angalia, Amri Kumi zilitoka kwenye midomo Yake. Kutoka 20:1 inasema, “Mungu akanena Maneno haya yote, akisema ... [Amri Kumi zinafuata katika mstari wa 2-17].”

**Jibu:** Hapana, kwa kweli! Haiwezekani kabisa kwa sheria yoyote ya Mungu ya maadili kubadilika kamwe. Amri zote Kumi ni za lazima leo.

Paulo na mitume wengine waliitakasa Sabato ya siku ya saba ya Mungu.

**6. Je, mitume waliitunza Sabato?**

“Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia kwao, akahojiana nao kwa maneno ya Maandiko Sabato tatu.” Matendo 17:2 . “Paulo na wenzake ... waliingia katika sinagogi siku ya Sabato, wakaketi.” Matendo 13:13 , 14 . “Siku ya Sabato tukatoka nje ya mji, tukaenda kando ya mto, mahali palipopagwa kusali, tukaketi, tukasema na wanawake waliokusanyika huko. Matendo 16:13 . “Naye [Paulo] alijadiliana katika sinagogi kila Sabato, akiwavuta Wayahudi na Wagiriki.” Matendo 18:4 .

**Jibu:** Ndiyo, kitabu cha Matendo ya Mitume kinaweka wazi kwamba Paulo na kanisa la kwanza waliitunza Sabato.

Mitume waliwafundisha Mataifa kuitakasa Sabato.

**7. Je, Mataifa pia waliabudu siku ya Sabato?**

*Mungu aliiamuru hivi:*

“Heri mtu yule ... aishikaye Sabato asiitie unajisi.” *“Tena wageni, watakaojiunga na Bwana,… kila mtu aishikaye Sabato asiitie unajisi,* na kulishikamana na agano Langu; hao hao nitawaleta katika mlima Wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika maisha Yangu. nyumba ya sala ... kwa maana nyumba Yangu itaitwa nyumba ya

sala kwa *watu wote* ." Isaya 56:2 , 6 , 7 , mkazo umeongezwa.

*Mitume walifundisha hivi:*

"Na Wayahudi walipotoka katika sinagogi, *watu wa mataifa wakawasihi wahubiriwe Maneno hayo Sabato iliyofuata* ." "Siku ya Sabato iliyofuata, karibu mji wote ukakusanyika ili kusikia Neno la Mungu." Matendo 13:42 , 44 , mkazo umeongezwa. "Akatoa hoja zake katika sinagogi kila Sabato, akiwavuta Wayahudi na Wagiriki." Matendo 18:4 .

**Jibu:** Mitume katika kanisa la kwanza la Agano Jipya hawakutii tu amri ya Sabato ya Mungu, bali pia waliwafundisha Mataifa walioongoka kuabudu siku ya Sabato. Kamwe hawarejelei Jumapili kama siku takatifu.

Sabato haikubadilishwa kuwa Jumapili wakati wa ufufuo wa Yesu.

**8. Lakini je, Sabato haikubadilishwa kuwa Jumapili wakati wa kifo au ufufuo wa Kristo?**

**Jibu:** Hapana, hakuna dokezo hata la kwa mbali zaidi kwamba Sabato ilibadilishwa wakati wa kifo au ufufuo wa Kristo. Biblia inafundisha kinyume kabisa. Tafadhali pitia kwa makini ushahidi ufuatao:

**A. Mungu aliibariki Sabato.**

"Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa." Kutoka 20:11 . "Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa." Mwanzo 2:3 .

**B. Kristo alitarajia watu Wake wangeendelea kushika Sabato katika mwaka wa 70 BK wakati Yerusalemu ilipoharibiwa.**

Akijua vyema kwamba Yerusalemu ingeangamizwa na Roma mwaka wa 70 BK, Yesu aliwaonya wafuasi Wake wa wakati huo, akisema, "Lakini ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya S*abato* . Mathayo 24:20 , mkazo umeongezwa. Yesu aliweka wazi kwamba alikusudia Sabato itunzwe hata miaka 40 baada ya kufufuka kwake. Kwa kweli, hakuna madokezo popote katika Maandiko kwamba Yesu, Baba Yake, au mitume waliwahi (wakati wowote, chini ya hali yoyote) kubadilisha Sabato takatifu ya siku ya saba kuwa siku nyingine yoyote.

**C. Wanawake waliokuja kuutia mafuta mwili wa Kristo waliitunza Sabato. Yesu alikufa "siku iliyotangulia sabato" ( Marko 15:37 , 42 ), ambayo sasa inaitwa Ijumaa Kuu.**

Wanawake walitayarisha manukato na marhamu ili kuupaka mwili Wake, kisha "wakapumzika siku ya Sabato kama ilivyoamriwa." Luka 23:56 . Ni "Sabato ilipokwisha kupita" ( Marko 16:1 ) ambapo wanawake walikuja "siku ya kwanza ya juma" ( Marko 16:2 ) ili kuendeleza kazi yao yenye kuhuzunisha. Walipata "Yesu alifufuka mapema siku ya kwanza ya juma" (mstari wa 9), ambayo kwa kawaida huitwa Jumapili ya Pasaka. Tafadhali kumbuka kwamba Sabato "kulingana na

amri" ilikuwa siku iliyotangulia Jumapili ya Pasaka, ambayo sasa tunaiita Jumamosi.

**D. Mfuasi wa Kristo, Luka, aliandika vitabu viwili vya Biblia, Luka na Matendo.** Anasema kwamba katika kitabu cha Luka aliandika kuhusu "mafundisho yote" ya Yesu ( Matendo 1:1-3 ). Lakini hakuandika kamwe kuhusu utunzaji wa Jumapili au mabadiliko ya Sabato.

Kila mtu katika ufalme wa milele wa Mungu ataitakasa Sabato.

**9. Baadhi ya watu husema Sabato itawekwa katika dunia mpya ya Mungu. Je, hii ni sahihi?**

"Maana kama vile mbingu mpya na nchi mpya, nitakazofanya, zitakavyokaa mbele Zangu, asema Bwana, ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa. Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya, na tangu Sabato hata Sabato, wote wenye mwili watakuja kuabudu mbele Zangu, asema Bwana. Isaya 66:22 , 23 .

**Jibu:** Ndiyo, Biblia inasema watu waliookolewa wa nyakati zote wataitunza Sabato katika dunia mpya.

Siku ya Bwana ni Sabato, si Jumapili.

**10. Lakini je, Jumapili si siku ya Bwana?**

Iiteni sabato siku ya furaha, takatifu ya Bwana. Isaya 58:13 . "Kwa maana Mwana wa Adamu Ndiye Bwana wa siku ya sabato." Mathayo 12:8 .

**Jibu:** Biblia inazungumza kuhusu "siku ya Bwana" katika Ufunuo 1:10, kwa hiyo Bwana ana siku maalum. Lakini hakuna mstari wa Maandiko unaorejelea Jumapili kuwa siku ya Bwana. Badala yake, Biblia hutambulisha waziwazi Sabato kuwa siku ya Bwana. Siku pekee iliyowahi kubarikiwa na Bwana au kudaiwa na Yeye kuwa siku Yake takatifu ni Sabato ya siku ya saba.

Yesu alianzisha ubatizo--sio utunzaji wa Jumapili--kwa heshima ya ufufuo Wake.

**11. Je, sistahili kushika Jumapili kwa heshima ya ufufuo wa Kristo?**

"Hamjui ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti Yake? Basi tulizikwa pamoja Naye kwa njia ya ubatizo katika mauti Yake, ili kama vile Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba; vivyo hivyo na sisi nasi tuenende katika upya wa uzima.Maana ikiwa tumeunganishwa katika mfano wa mauti Yake, tutakuwa katika mfano wa kufufuka Kwake; mwili wa dhambi upate kuharibiwa, ili tusitumikie dhambi tena." Warumi 6:3-6 .

**Jibu:** Hapana! Si zaidi ya vile ungetunza Ijumaa kwa heshima ya kusulubiwa. Kristo alitoa agizo la ubatizo kwa heshima ya kifo Chake, kuzikwa, na ufufuo Wake. Biblia haipendekezi kamwe kushika Jumapili kwa heshima ya ufufuo (au kwa sababu nyingine yoyote, kwa jambo hilo). Tunamheshimu Kristo kwa kumtii ( Yohana 14:15 )--si kwa kuweka matakwa ya mwanadamu badala ya Yake.

Watu waliopotoka walikuwa na ujasiri wa kuibadilisha Jumapili badala ya Sabato ya sheria ya Mungu.

**12. Vema, kama utunzaji wa Jumapili haumo katika Biblia, lilikuwa wazo la nani basi?**

"Naye ataazimu kubadili majira na sheria." Danieli 7:25 , UV.* "Hivi ndivyo mmeibatilisha amri ya Mungu kwa mapokeo yenu." "Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu." Mathayo 15:6 , 9 . Makuhani wake wameihalifu sheria Yangu. "Na manabii wake wamewapaka chokaa kisicho na joto, ... wakisema, Bwana MUNGU asema hivi; wakati Bwana hakunena." Ezekieli 22:26 , 28 .

**Jibu:** Watu waliopotoka wa miaka mingi iliyopita walitangaza kwamba siku takatifu ya Mungu ilibadilishwa kutoka Sabato hadi Jumapili. Mungu alitabiri jambo hilo lingetukia, nalo lilifanyika. Kosa hili lilipitishwa kwa kizazi chetu kisicho na mashaka kama Ukweli wa injili. Utunzaji wa Jumapili ni desturi ya watu ambao hawajavuviwa na huvunja sheria ya Mungu, inayoamuru kushika Sabato. Mungu pekee Ndiye anayeweza kuifanya siku kuwa takatifu. Mungu aliibariki Sabato, na Mungu anapobariki, hakuna mtu anayeweza "kuigeuza." Hesabu 23:20 .

Kuibadili Sabato kuwa Jumapili ni dharau kwa Mungu kwa sababu inajaribu kubadilisha sheria Yake takatifu.

**13. Lakini je, si hatari sana kuchezea sheria ya Mungu?**

"Msiliongeze Neno niwaamurulo, wala msipunguze Neno lolote, mpate kuzishika amri za Bwana, Mungu wenu." Kumbukumbu la Torati 4:2 . "Kila Neno la Mungu ni safi.... Usiongeze neno katika Maneno Yake, asije akakulaumu, ukaonekana kuwa mwongo." Methali 30:5 , 6 .

**Jibu:** Mungu amekataza kwa hakika kwa watu kubadilisha sheria Yake kwa kufuta au kuongeza. Kuichezea sheria takatifu ya Mungu kwa njia yoyote ile ni moja ya mambo ya kutisha na hatari sana ambayo mtu anaweza kufanya.

Sabato ni ishara ya uwezo wa Mungu wa kuumba na kukomboa.

**14. Kwa nini Mungu aliifanya Sabato hata hivyo?**

*A. Ishara ya Uumbaji.*

"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase." "Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa." Kutoka 20:8 , 11 .

*B. Ishara ya ukombozi na utakaso.*

"Tena naliwapa Sabato Zangu, ziwe ishara kati ya mimi na wao, wapate kujua ya kuwa Mimi, Bwana, Ndimi niwatakasaye." Ezekieli 20:12 .

**Jibu:** Mungu alitoa Sabato kama ishara mbili: (1) Ni ishara kwamba aliumba

ulimwengu katika siku sita halisi za saa 24, na (2) pia ni ishara ya uwezo mkuu wa Mungu wa kuwakomboa na kuwatakasa wanadamu. Hakika kila Mkristo atapenda Sabato kama ishara ya thamani ya Mungu ya Uumbaji na ukombozi ( Kutoka 31:13 , 17 ; Ezekieli 20:12 , 20 ). Ni dharau kubwa kwa Mungu, kwa watu kuikanyaga Sabato Yake. Katika Isaya 58:13 , 14 , Mungu anasema wote ambao wangebarikiwa lazima kwanza waondoe miguu yao kutoka kwa Sabato Yake.

Kuvunja amri yoyote ya sheria ya Mungu ni dhambi.

**15. Kushika Sabato ni muhimu kadiri gani?**

"Dhambi ni uvunjaji wa sheria." 1 Yohana 3:4 . "Mshahara wa dhambi ni mauti." Warumi 6:23. "Yeyote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote." Yakobo 2:10. "Kristo Naye aliteswa kwa ajili yetu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo Zake." 1 Petro 2:21 . "Amekuwa chanzo cha wokovu wa milele kwa wote wanaomtii." Waebrania 5:9 .

**Jibu:** Ni suala la uzima na kifo. Utunzaji wa Sabato umewekwa katika amri ya nne ya sheria ya Mungu. Kuvunja kwa makusudi mojawapo ya Amri Kumi ni dhambi. Wakristo watafuata kwa furaha kielelezo cha Kristo cha kushika Sabato. Usalama wetu pekee ni kujifunza Biblia kwa bidii, "tukigawanya kwa usahihi Neno la Kweli."

2 Timotheo 2:15 . Ni lazima tuwe na usaidizi chanya wa Maandiko kwa kila mazoea ya Kikristo tunayofuata.

Mungu atamwaga ghadhabu Yake juu ya viongozi wa kidini ambao kwa makusudi wanapuuza Sabato Yake.

**16. Mungu anahisije kuhusu viongozi wa kidini wanaopuuza Sabato?**

"Makuhani wake wameihalifu sheria Yyangu, nao wametia unajisi vitu Vyangu vitakatifu; "Kwa hiyo nimemwaga ghadhabu Yangu juu yao." Ezekieli 22:26 , 31 .

**Jibu:** Kwa kuficha macho yao wasiione Sabato ya Kkweli ya Mungu, viongozi wa kidini wanamchukiza Mungu wa mbinguni. Mungu anaahidi adhabu kwa wachungaji hao wa uwongo. Mamilioni ya watu wamepotoshwa katika suala hili. Mungu hawezi kulichukulia kirahisi. Yesu aliwashutumu Mafarisayo kwa kujifanya wanampenda Mungu huku wakibatilisha mojawapo ya Amri Kumi kwa mapokeo yao ( Marko 7:7-13 ).

Kila mtu anayeingia mbinguni na kula matunda ya mti wa uzima ataitakasa Sabato ya Mungu.

**17. Je, kushika Sabato kunaniathiri mimi binafsi?**

"Mkinipenda, mtazishika amri Zangu." Yohana 14:15 . "Basi basi, kila mmoja wetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu." Warumi 14:12 . "Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi." Yakobo 4:17 . "Heri wazishikao amri Zake, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango Yake." Ufunuo 22:14 . "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu." Ufunuo 14:12 .

**Jibu:** Ndiyo, kwa vyovyote vile, Sabato ni Sabato *yako* . Mungu aliifanya kwa ajili *yako,* na ukimpenda utaishika, kwa sababu ni mojawapo ya amri Zake. Upendo bila kushika amri hakuna upendo hata kidogo ( 1 Yohana 2:4 ). Lazima ufanye uamuzi. Huwezi kuikwepa. Hakuna anayeweza kukusamehe. Wewe mwenyewe utajibu mbele za Mungu juu ya jambo hili muhimu zaidi. Mungu anakuomba umpende na kumtii sasa!

**18. Niko tayari kufuata mfano wa Yesu wa kushika Sabato.**

**Jibu:**

## MASWALI YA KUCHEUA NA KUTAFAKARI

**1. Lakini je, Sabato si ya Wayahudi pekee?**

Hapana. Yesu alisema, "Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu." Marko 2:27. Si kwa ajili ya Wayahudi pekee, bali ni kwa ajili ya wanadamu--wote wanaume na wanawake kila mahali. Taifa la Kiyahudi halikuwepo mpaka baada ya miaka 2,500 ya Sabato kufanywa.

**2. Je, Matendo 20:7-12 si uthibitisho kwamba wanafunzi waliitunza Jumapili kama siku takatifu?**

Kulingana na Biblia, kila siku huanza jua linapotua na kuishia machweo yanayofuata ( Mwanzo 1:5 , 8 , 13 , 19 , 23 , 31 ) (Mambo ya Walawi 23:32 ) na sehemu ya giza ya siku inakuja kwanza. Siku alivyoiumba Mungu ilianza jua likitua na kuisha jua likitua. Mambo ya siku kuisha na kuanza saa sita ya usiku yalianzishwa na serikali ya Rumi ikitawala dunia. Kwa hiyo Sabato huanza Ijumaa jioni wakati wa machweo ya jua na kuisha Jumamosi jioni wakati wa machweo ya jua. Mkutano huu wa Matendo 20 ulifanyika katika sehemu ya giza ya Jumapili, au katika kile tunachokiita sasa Jumamosi usiku. Huanza kama inavyosema Matendo 20:7 hivi: "Siku ya Jumamosi usiku katika kusanyiko letu ..."

Ulikuwa mkutano wa Jumamosi usiku, nao uliendelea hadi usiku wa manane. Paulo alikuwa katika safari ya kuaga na alijua hatawaona watu hawa tena kabla ya kifo chake (mstari 25). Si ajabu kwamba alihubiri kwa muda mrefu sana! (Hakuna ibada ya kawaida ya juma ambayo ingedumu usiku kucha.) Paulo alikuwa "tayari kuondoka kesho yake." "Kumega mkate" hakumaanishi katika "siku takatifu" na hakuna muhimu wowote, kwa sababu walimega mkate kila siku ( Matendo 2:46 ). Hakuna dalili hata kidogo katika fungu hili la Maandiko kwamba siku ya kwanza ni takatifu, wala kwamba Wakristo hawa wa awali waliiona hivyo. Wala hakuna ushahidi wa mbali kabisa kwamba Sabato ilikuwa imebadilishwa. Kwa bahati mbaya, mkutano huu labda umetajwa katika Maandiko kwa sababu tu ya muujiza wa kumfufua Eutiko baada ya kuanguka hadi kufa kutoka kwenye dirisha la ghorofa ya tatu. Katika Ezekieli 46:1 , Mungu anarejelea Jumapili kama moja ya "siku za kazi" sita.

**3. Je, 1 Wakorintho 16:1, 2 haisemi kuhusu matoleo ya shule ya Jumapili?**

Hapana, hakuna marejeleo hapa ya mkutano wa hadhara. Pesa hizo zilipaswa kuwekwa faragha nyumbani. Njaa ilikuwa ikiendelea Yudea ( Warumi 15:26 ; Matendo 11:26-30 ), na Paulo alikuwa anaandika ili kuyaomba makanisa ya Asia Ndogo kuwasaidia ndugu zao waliokumbwa na njaa. Wakristo hawa wote waliitakasa Sabato, kwa hiyo Paulo alipendekeza kwamba siku ya Jumapili asubuhi (ambayo ilikuwa ni wakati wa kulipa bili na kuweka mahesabu sawa), baada ya Sabato kwisha, waweke kando kitu kwa ajili ya ndugu zao wenye mahitaji ili pesa iwepo wakati atakapokuja. . Ilipaswa kufanywa kwa faragha au, kama *La Santa Biblia* (tafsiri ya Kihispania) inavyosema, "nyumbani." Angalia pia kwamba hakuna rejea hapa kwa Jumapili kama siku takatifu. Kwa kweli, Biblia haiamuru au hata kupendekeza kushika Jumapili.

**4. Lakini je, muda haujapotea na siku za juma kubadilika tangu wakati wa Kristo?**
Hapana! Encyclopedia/Ensaiklopidia na vitabu vya marejeo vinavyotegemeka huonyesha wazi kwamba siku yetu ya saba ndiyo ileile ambayo Yesu aliitakasa. Ni suala rahisi la utafiti.

**5. Lakini je, Yohana 20:19 si rekodi ya wanafunzi kuanzisha Utunzaji wa Jumapili kwa heshima ya ufufuo?**

Kinyume chake, wanafunzi wakati huu hawakuamini kwamba ufufuo ulifanyika ( Marko 16:14 ). Walikuwa wamekutana huko "kwa kuwaogopa Wayahudi" na walikuwa wamefunga milango. Yesu alipotokea katikati yao, Naye aliwakemea "kwa sababu hawakuwaamini wale waliomwona baada ya kufufuka Kwake. Hakuna maana basi kwamba walihesabu Jumapili kuwa siku takatifu kama waliogopa! Maandiko manane tu katika Agano Jipya yanataja siku ya kwanza ya juma; hakuna hata moja kati yao inayodokeza kwamba ni takatifu.

**6. Je, Wakolosai 2:14-17 haiondoi Sabato ya siku ya saba?**

Hapana kabisa. Inarejelea tu sabato ambazo zilikuwa "kivuli cha mambo yajayo" na sio Sabato ya siku ya saba. Kulikuwa na siku saba za kila mwaka takatifu, au sikukuu, katika Israeli ya kale ambazo ziliitwa pia sabato. Hizi zilikuwa ni nyongeza, au "kando ya Sabato za Bwana" ( Mambo ya Walawi 23:38 ), au Sabato ya siku ya saba. Haya yote yalitangulia, au yalionyesha, msalaba na kuishia msalabani. Sabato ya Mungu ya siku ya saba ilifanywa kabla ya dhambi kuingia, na kwa hiyo haikuweza kuwa kivuli chochote kuhusu ukombozi kutoka kwa dhambi. Ndiyo maana Wakolosai sura ya 2 inatofautisha na kutaja hasa sabato ambazo zilikuwa "kivuli." Sabato hizi saba za mwaka ambazo zilikomeshwa zimeorodheshwa katika Mambo ya Walawi sura ya 23.

**7. Kulingana na Warumi 14:5 , siku tunayoitunza kama takatifu ni suala la maoni ya kibinafsi, sivyo?**

Angalia kwamba sura nzima inahusu kuhukumiana (Mistari ya 4, 10, 13). Suala hapa si juu ya Sabato ya siku ya saba, ambayo ilikuwa ni sehemu ya sheria kuu ya maadili, bali ni kuhusu sikukuu za kila mwaka za sheria ya maadhimisho (ceremonial

laws zilizohusu kafara za wanyama). Wakristo Wayahudi walikuwa wakiwahukumu Wakristo wasio Wayahudi kwa sababu hawakuzitunza. Paulo anasema kwa urahisi, "Msihukumu ninyi kwa ninyi. Sheria hiyo ya sherehe haifungi tena."

## MASWALI YA CHEMSHA BONGO, KWIZZ

**1. Yesu aliitunza (1)**
Jumapili ya _____ kama siku takatifu.
_____ Sabato ya siku ya saba takatifu.
_____ Kila siku nyingine takatifu.

**2. Siku ya Bwana ni (1)**
_____ Jumapili, siku ya kwanza ya juma.
_____ Sabato, siku ya saba ya juma.
_____ Siku yoyote tunayoweka wakfu kwa Bwana.

**3. Sabato ilifanywa (1)**
_____ Kwa Wayahudi pekee.
_____ Na Mungu katika Uumbaji kwa wanaume na wanawake wote kila mahali kwa wakati wote.
_____ Kwa watu walioishi nyakati za Agano la Kale pekee.

**4. Badiliko kutoka Sabato kwenda Jumapili lilifanywa na (1)**
_____ Kristo.
_____ Mitume.
_____ Watu wapotofu.

**5. Sheria ya Mungu, ambayo inajumuisha amri ya Sabato, (1)**
_____ haifanyi kazi tena leo.
_____ Kamwe haiwezi kubadilika. Bado inatufungua na ina mashiko leo.
_____ Iliisha kwa kifo cha Kristo.

**6. Katika kanisa la Agano Jipya, Watu wa mataifa walioongoka na mitume (1)**
_____ Waliadhimisha Jumapili kama siku takatifu.
_____ Walifundishwa kwamba siku yoyote itatosha kuwa siku takatifu ikiwa wewe ni mwaminifu.
_____ Walishika Sabato.

**7. Sabato (1)**
_____ Iliishia msalabani.
_____ Itaisha wakati wa kuja kwa Yesu mara ya pili.
_____ Itahifadhiwa katika ufalme mpya wa milele wa Mungu na waliokombolewa wa nyakati zote.

**8. Kwa kuwa Sabato ni sehemu ya sheria ya Mungu, kuvunja Sabato ni (1)**
_____ Hakuna haja ya kutaji tangu kifo cha Kristo.
_____ Dhambi hatari kwa sababu inakanyaga vitu vitakatifu.

_____ Hakuna umuhimu leo.

**9. Wote wanaompenda na kumfuata Yesu kwa kweli (1)**
_____Wataishika Sabato, kama Yesu alivyoitunza.
_____ Wataweka kila siku nyingine kuwa takatifu.
_____ Watashika Jumapili kama siku takatifu.

**10. Sabato ni (1)**
_____ Jumapili, siku ya kwanza ya juma.
_____ Jumamosi, siku ya saba ya juma.
_____ Siku yoyote tunayoweka wakfu kwa Mungu.

**11. Utunzaji wa Jumapili (1)**
_____ Ni uvumbuzi wa wanadamu ambao ulitabiriwa katika Biblia.
_____ Ndio mpango wa Mungu kwa siku ya leo.
_____ Ulianzishwa wakati wa ufufuo wa Kristo na kuidhinishwa siku ya Pentekoste.

**12. Utunzaji wa Sabato ni (1)**
_____ Ni Ishara ya ushupavu wa sheria.
_____Ni Muhimu kwa Wayahudi pekee.
_____ Ni Ishara ya Mungu yenye sehemu mbili ya Uumbaji na ukombozi.

## Ukombozi wa Mwisho

### Somo la 8

Sio hekaya ya Abunuwasi - siku moja, wewe unaweza kuwa huru kutokana na maudhi, njaa, upweke, uhalifu, na machafuko yanayoathiri ulimwengu leo. Je! hilo halionekani kuwa la ajabu? Lakini hatakuwa kiongozi fulani wa kidunia mwenye haiba ambaye atakukomboa... hapana, Yeye ni mkuu zaidi kuliko huyo! Yesu anakuja hivi karibuni, lakini kuna maoni mengi potofu yanayojulikana kuhusu jinsi atakavyokuja. Kwa hiyo chukua dakika chache kuelewa kile ambacho Biblia inasema hasa kuhusu ujio wa pili ili usiachwe nyuma!

Yesu alifundisha kwamba atarudi duniani mara ya pili.

**1. Je, Yesu atarudi hapa duniani mara ya pili? Je, tunaweza kuwa chanya na jambo hilo?**

“Kristo ... atatokea mara ya pili.” Waebrania 9:28 .

“Nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena.” Yohana 14:3 .

**Jibu:** Ndiyo! Katika Mathayo 26:64 , Yesu alishuhudia chini ya kiapo kwamba angerudi duniani tena. Kwa kuwa Maandiko hayawezi kuvunjwa ( Yohana 10:35), huu ni uthibitisho chanya. Amini kama inavyosomeka. Ni dhamana ya Kristo Mwenyewe binafsi.

Yesu alisema atarudi duniani katika mawingu.

**2. Yesu atarudi mara ya pili kwa namna gani?**

"Walipotazama akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. Na walipokuwa wakitazama mbinguni, alipokuwa akipanda, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye mavazi meupe; wakasema, Enyi watu wa mataifa. Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Yesu Huyu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda Zake mbinguni. Matendo 1:9-11 .

**Jibu:** Maandiko yanaahidi kwamba Yesu atarudi hapa duniani kwa namna ile ile aliyoiacha wakati wa kupaa Kwake--kwa kuonekana, halisi, kimwili na uso kwa uso au kibinafsi. Mathayo 24:30 inasema, "Watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi." Atakuja mawinguni kihalisi, akiwa mtu binafsi mwenye mwili wa nyama na mifupa ( Luka 24:36-43 , 50 , 51 ), na kuja Kwake kutaonekana. Maandiko yako wazi juu ya mambo haya.

Kila mtu anayeishi duniani atamwona Yesu atakaporudi mara ya pili.

**3. Je, ujio wa pili wa Kristo utaonekana kwa watu wote au kwa kundi teule pekee?**

"Tazama, Yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona." Ufunuo 1:7.

"Kwa maana kama vile umeme unavyotokea mashariki na kuangaza hata magharibi, ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu. Mathayo 24:27 .

**Jibu:** Kila mwanamume, mwanamke, na mtoto anayeishi ulimwenguni Yesu atakaporudi atamwona wakati wa kuja Kwake mara ya pili. Mwangaza wa kuja Kwake utaenea kutoka upeo wa macho hadi upeo wa macho, na angahewa itajaa utukufu mwingi kama umeme. Hakuna atakayeweza kujificha. Kila nafsi hai italazimika kumkabili Kristo. Kristo hakuacha mwanya wa shaka au kutokuelewaka.

***Kumbuka:*** *Unyakuo wa siri unaoaminika na kufundishwa na watu wengi leo haumo katika Biblia. Ni ubunifu wa mwanadamu tu. Wala ujio wa pili sio wa kiroho wa Yesu kuingia moyoni wakati wa kuongoka. Huitukii mtu anapokufa, wala si ya kitamathali, kwamba utadhihirishwa na hali bora zaidi za ulimwengu. Nadharia hizi zote zimetoka kwa mwanadamu. Kuja kwa mara ya pili kutakuwa kunaonekana kwa macho yaani halisi, ulimwenguni pote, atatokea mwenyewe binafsi mawinguni ili kuuleta ulimwengu huu kwenye mwisho wake na kuwazawadia au kuwaadhibu wanaume na wanawake wote.*

Malaika wote wa mbinguni watakuwa pamoja na Yesu wakati wa kuja Kwake mara ya pili.

**4. Ni nani watakaokuja pamoja na Yesu wakati wa kuja Kwake mara ya pili, na kwa nini?**

"Wakati Mwana wa Adamu atakapokuja katika utukufu Wake, na malaika watakatifu wote pamoja Naye, ndipo atakapoketi juu ya kiti cha utukufu Wake." Mathayo 25:31 .

**Jibu:** Malaika wote wa mbinguni watakuja pamoja na Yesu wakati wa kuja Kwake mara ya pili. Wingu linapokaribia dunia, Yesu atatuma malaika Zake, na watakusanya pamoja watu wote waadilifu haraka ili kujitayarisha kwa ajili ya safari ya kurudi mbinguni (Mathayo 24:31 ).

Yesu atawachukua watu Wake kwenda mbinguni na kuwarudishia kila kitu ambacho Adamu na Hawa walipoteza.

**5. Kusudi la kuja kwa Yesu mara ya pili katika dunia hii ni nini?**

"Na tazama, Naja upesi, na ujira Wangu u pamoja Nammi, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo." Ufunuo 22:12 .

"Nitakuja tena niwakaribishe Kwangu; ili nilipo Mimi, nanyi mwepo." Yohana 14:3 .

"Naye atamtuma Yesu Kristo ... ambaye mbingu lazima zimpokee hata nyakati za kufanywa upya vitu vyote." Matendo 3:20 , 21 .

**Jibu:** Yesu anarudi duniani ili kuwathawabisha watu Wake kama alivyoahidi na kuwapeleka kwenye makao mazuri aliyowaandalia. Atawarudishia watu Wake furaha na utukufu wote wa Edeni ambao Adamu na Hawa walipoteza kwa kufanya dhambi. Kuja Kwake mara ya pili kutakomesha enzi hii ya uovu.

Watoto wadogo waliochukuliwa kutoka kwa wazazi wao kwa kifo watarudishwa kwao katika ujio wa pili wa Yesu.

**6. Ni nini kitakachowapata wenye haki Yesu atakapokuja mara ya pili?**

"Kwa maana Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni ... na waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza; kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; tuko pamoja na Bwana daima." 1 Wathesalonike 4:16 , 17 .

"Sisi sote tutabadilishwa, ... na wafu watafufuliwa wasiwe na uharibifu. Kwa maana ... huu wa kufa lazima uvae kutokufa." 1 Wakorintho 15:51-53 .

"Tunamtazamia ... Bwana Yesu Kristo: ambaye ataubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili Wake wa utukufu." Wafilipi 3:20 , 21 .

**Jibu:** Wafu wenye haki watafufuliwa kutoka makaburini mwao, wakipewa miili kamilifu, isiyoweza kufa kama ile ya Kristo, na kunyakuliwa juu mawinguni ili kumlaki Bwana. Ndipo wenye haki walio hai pia watapewa miili kama ya Kristo na kunyakuliwa ili kumlaki Bwana hewani. Na Yesu atawachukua wenye haki mbinguni pamoja Naye.

Kumbuka kwamba Yesu hagusi dunia wakati wa kuja Kwake mara ya pili. Watakatifu wanakutana Naye "hewani." Kwa hiyo watu wa Mungu watapuuza ripoti yoyote inayosema kwamba Kristo yuko Bujumbura, Mwanza, Goma, Nairobi, n.k. Makristo wa uwongo watatokea na kufanya miujiza duniani ( Mathayo 24:23-27 ), lakini Yesu atabaki katika mawingu juu ya dunia. katika kuja Kwake mara ya pili.

Waovu watauawa Yesu atakapokuja mara ya pili.

**7. Ni nini kitakachowapata watu waovu Yesu atakapokuja tena?**

“Kwa pumzi ya midomo Yake atawaua waovu.” Isaya 11:4 .

“Na hao waliouawa na Bwana watakuwa siku hiyo, toka upande mmoja wa dunia hata upande wa pili wa dunia.” Yeremia 25:33 .

**Jibu:** Waovu watauawa na Yesu.

Matetemeko ya ardhi ya leo ni madogo kwa kulinganisha na tetemeko kubwa la ardhi wakati wa kuja kwa Yesu.

**8. Kuja kwa pili kwa Kristo kutaathirije dunia yenyewe?**

“Kukawa na tetemeko kuu la nchi, ambalo tangu wanadamu kuwako juu ya nchi ambalo halijakuwa namna hiyo, na tetemeko kuu namna hii. “Kila kisiwa kikakimbia, na milima haikuonekana.” Ufunuo 16:18 , 20 .

“Nikatazama, na tazama, mahali pa matunda palikuwa ni nyika, na miji yake yote ilikuwa imebomoka mbele za uso wa Bwana.” Yeremia 4:26 .

“Bwana huifanya dunia kuwa tupu, na kuifanya ukiwa.” “Nchi itakuwa tupu kabisa.” Isaya 24:1 , 3 .

**Jibu:** Nchi itashikwa na tetemeko kubwa la ardhi wakati wa kuja Kwake Bwana. Tetemeko hili la ardhi litakuwa la uharibifu mkubwa kiasi kwamba litaiacha dunia katika hali ya uharibifu kabisa.

Mamilioni ya Wakristo walikufa wakati wa Enzi za Giza. Wengi walichomwa motoni.

**9. Je, Biblia inatoa habari hususa kuhusu ukaribu wa kuja kwa pili kwa Kristo?**

**Jibu:** Ndiyo, inafanya! Na Yesu Mwenyewe alisema, “Mtakapoona mambo haya yote, tambueni ya kuwa Yu karibu, milangoni.” Mathayo 24:33 . Bwana aliweka ishara njiani kote kutoka kupaa Kwake hadi kuja Kwake mara ya pili. Hizi zimeorodheshwa hapa chini. Jifunze kwa uangalifu.

A. Kuangamizwa kwa Yerusalemu

**Unabii: “Hatasalia jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa.” “Walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani.” Mathayo 24:2 , 16 .**

Utimizo: Yerusalemu iliharibiwa mwaka wa 70 BK na Jemedari wa Kirumi Tito.

B. Mateso Makuu, au

**Unabii wa Dhiki: “Kwa maana wakati huo kutakuwa na dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu.” Mathayo 24:21 .**

Utimizo: Unabii huu unaelekeza hasa kwenye kipindi kirefu cha dhiki kilichotukia wakati wa Enzi za Giza na kuchochewa na kanisa lililoasi. Ulidumu zaidi ya miaka

1,000. Zaidi ya Wakristo milioni 50 waliuawa kwa ajili ya imani yao katika kipindi hiki cha dhiki ya kutisha. Mwandishi mmoja asema kanisa lililoasi imani "limemwaga damu nyingi zaidi isiyo na hatia kuliko taasisi nyingine yoyote ambayo imewahi kuwako kati ya wanadamu."

C. Jua Limegeuka Kuwa Giza Unabii**:**

**"Mara baada ya dhiki ya siku zile jua litatiwa giza." Mathayo 24:29 .**

Utimizo: Hilo lilitimizwa kwa siku ileya giza lisilo la kawaida mnamo Mei 19, 1780. Haikuwa kupatwa kwa jua. Timothy Dwight anasema, "Tarehe 19 Mei, 1780, ilikuwa siku ya giza ya ajabu. Mishumaa iliwashwa katika nyumba nyingi, ndege walikuwa kimya na kutoweka, na kuku walistaafu ili kwenda kulala ... Maoni ya jumla yaliyotawala ilikuwa ni kwamba siku ya hukumu ilikuwa karibu." Imenukuliwa katika *Mikusanyo ya Kihistoria ya Connecticut,* iliyoandaliwa na John Warner Barber ( toleo la 2. New Haven: Durrie & Peck na JW Barber, 1836) uk. 403.

D. Mwezi Kugeuzwa Damu

**Unabii: "Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na itishayo." Yoeli 2:31 .**

Utimizo: Mwezi ukawa mwekundu kama damu usiku wa "siku ya giza," Mei 19, 1780. Milo Bostick katika *Stone's History of Massachusetts* anasema, "Mwezi uliokuwa mzima/mpevu, ulikuwa na mwonekano wa damu."

Mvua kubwa ya nyota ilifanyika mnamo Novemba 13, 1833.

E. Nyota Zinaanguka kutoka Mbinguni
**Unabii: "Na nyota zitaanguka kutoka mbinguni." Mathayo 24:29 .**

Utimizo: Mvua kubwa ya nyota ilifanyika usiku wa Novemba 13, 1833. Kulikua na mwanga mkali sana hivi kwamba gazeti lingeweza kusomwa mitaani. Mwandishi mmoja asema, "Kwa karibu masaa manne anga lilikuwa linawaka ."* Watu walifikiri kwamba mwisho wa ulimwengu ulikuwa umefika. Angalia katika hili. Ni jambo la kuvutia zaidi, nayo ni ishara ya kuja kwa Kristo.

* Peter A. Millman, "Kuanguka kwa Nyota," *Darubini,* 7 (May-Juni, 1940) 57.

F. Yesu Aja Katika Mawingu

**Unabii: "Ndipo itakapoonekana ishara ya Mwana wa Adamu mbinguni : ndipo kabila zote za dunia watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija katika mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Mathayo 24:30 .**

Utimizo: Hili ni tukio kubwa linalofuata. Uko tayari?

Ugomvi kati ya mtaji na kazi ni ishara ya ujio wa pili wa Yesu.

**10. Tunaweza kujua jinsi gani wakati tumefikia siku za mwisho kabisa za historia ya dunia? Je, Biblia inaeleza waziwazi ulimwengu na watu wake katika kizazi kilichopita?**

**Jibu:** Ndio, ni jambo la kweli. Tazama ishara maalum zifuatazo za siku za mwisho. Utashangaa. Na hizi ni baadhi tu ya ishara nyingi chanya zinazoonyesha kwamba tuko katika siku za mwisho za historia ya dunia.

A. Matatizo ya mtaji

**“Mshahara wa wakulima waliovuna mashamba yenu, mliozuiwa kwenu kwa hila, unalia; na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana.” “kuwa … mvumilivu … kwa kuwa kuja Kwake Bwana kunakaribia.” Yakobo 5:4 , 8 .**

Shida kati ya mtaji na kazi inatabiriwa kwa siku za mwisho. Kwa utimilifu, wasiliana na magazeti yako.

B. Vita na machafuko

**“Lakini mtakaposikia habari za vita na misukosuko, msitishwe; kwa maana hayo hayana budi kutukia kwanza.” Luka 21:9 .**

Vita na uharibifu wa misiba ya wenyewe kwa wenyewe unaathiri maelfu ya watu ulimwenguni pote. Ni kuja kwa Yesu tu upesi ndiko kutakomesha maumivu na uharibifu wa vita.

C. Machafuko, hofu, na misukosuko

**“Na kutakuwa … juu ya dunia dhiki ya mataifa, wakishangaa … Mioyo ya watu itazimia kwa hofu, na kwa kutazamia mambo yatakayoupata nchi.” Luka 21:25 , 26 .**

Hili linasikika kwa njia ya ajabu kama habari za mhariri kutoka gazeti la sasa kuhusu picha kamili ya ulimwengu leo na kuna mafundisho hapa: Sisi ni watu wa siku za mwisho kabisa za historia ya dunia. Hali ya wasiwasi iliyopo duniani leo isitushangaze. Kristo alitabiri. Jambo hili linapaswa kutushawishi kwamba kuja Kwake kumekaribia.

D. Kuongezeka kwa maarifa

**“Hata wakati wa mwisho … maarifa yataongezeka.” Danieli 12:4 .**

Enzi ya Maarifa/habari hufanya jambo hili liwe wazi sana. Hata akili yenye mashaka zaidi lazima ikubali kwamba ishara hii imetimizwa. Maarifa yanalipuka katika pande zote kila kukicha. Inasemekana kwamba asilimia 80 ya ujuzi wote ulimwenguni umetokezekea katika mwongo uliopita (miaka kumi)na kwamba asilimia 90 ya wanasayansi wote ambao wamewahi kuishi wako hai leo.

E. Watu wanaodhihaki na wakosoaji wa kidini wanaokengeuka kutoka kwenye Ukweli wa Biblia wamezidi kuongezeka

**"Siku za mwisho watakuja watu wenye kudhihaki." 2 Petro 3:3 . "Hawatakubali mafundisho yenye uzima … nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo." 2 Timotheo 4:3 , 4 .**

Sio vigumu kupata wenye dhihaka leo katika utimizo wa unabii huu. Hata viongozi wa kidini wanakana mafundisho ya Biblia yaliyo wazi ya Uumbaji, Gharika, Uuungu wa Kristo, ujio wa pili wa Kristo, na Kweli nyingine nyingi muhimu za Biblia. Saikolojia na mapokeo ya wasomi bandia yamechukua nafasi ya Biblia katika duru nyingi za kidini. Waelimishaji wa kilimwengu wanawafundisha vijana wetu kudhihaki rekodi ya Biblia ya Kweli hizi kuu na kuchukua nafasi ya Uibukaji na mafundisho mengine ya uongo ya mwanadamu kwa ajili ya mambo ambayo hakika yako wazi, na yaliyo sahili ya Neno Takatifu la Mungu. Kura ya maoni ya hivi majuzi iligundua kwamba ni asilimia mbili tu ya wanafunzi wanaosomea uchungaji Marekani, ndio wanaoamini katika ujio halisi wa pili wa Kristo.

F. Kushuka kwa maadili; kuporomoka kwa hali ya kiroho

**"Katika siku za mwisho … watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, … wasio na upendo wa asili, … wasiojizuia, … wenye kudharau walio wema, … wenye namna ya utauwa , lakini wakikana nguvu zake." 2 Timotheo 3:1-5 .**

Amerika iko katikati ya mzozo mkubwa. Watu kutoka nyanja zote za maisha wanasema hivyo. Kujiua kunakuwa suluhisho maarufu kwa shida za wanadamu. Viwango vya talaka vinapanda sana, na karibu ndoa moja kati ya mbili huishia katika mahakama ya talaka. Kizazi cha sasa kisicho na maadili, pamoja na kuhangaikia sana na ngono haramu na chafu, kina idadi ya washiriki wanaoongezeka kanisani kila kukicha, lakini hali ya kiroho ya Kweli inapungua, huku ni kutimia kwa unabii kuliko wazi na chanya kwa Neno la Mungu. Hakika utapata mshtuko ukiona orodha ya dhambi za siku za mwisho zilizoorodheshwa katika 2 Timotheo 3:1-5 Unaweza kuzipata hizi zikiwa zimeonyeshwa katika toleo lolote la gazeti lako la kila siku. Kuja kwa Bwana hakujazuia wimbi la uovu ambalo sasa linatawala ulimwengu.

G. Kutamani anasa

**"Siku za mwisho … watu watakuwa … wapenda anasa kuliko kumpenda Mungu." 2 Timotheo 3:1-4 .**

Ulimwengu umekuwa na wenda wazimu kwa raha na anasa. Asilimia ndogo tu ya wananchi wa miji yetu mikubwa huhudhuria ibada za kanisa mara kwa mara, lakini watu maelfu husongamana katika maeneo ya starehe. Marekani inatumia mabilioni kila mwaka kwa ajili ya kujifurahisha na "mambo madogomadogo na ya kipuuzi " tu (kwa kulinganisha) na matumizi kwa ajili ya kusaidia kazi ya Mungu. Wamarekani wenye wazimu wa kujifurahisha hupoteza mabilioni ya saa mbele ya simu au runinga katika kutimiza moja kwa moja unabii wa 2 Timotheo 3:4 .

H. Kuongezeka kwa uasi wa sheria, uhalifu wa umwagaji damu, na vurugu

**"Uovu utakuwa mwingi." Mathayo 24:12 . "Watu waovu na wadanganyifu watazidi kuwa waovu." 2 Timotheo 3:13 . "Nchi imejaa uhalifu wa umwagaji damu, na jiji limejaa jeuri." Ezekieli 7:23 .**

Ni wazi kabisa kwamba ishara hii imetimizwa. Uhalifu na uasi sheria vinaongezeka kwa kasi ya kushangaza. Watu wengi katika miji mikubwa hawajibu kengele za milango yao baada ya giza kuingia. Watawala wenye hekima zaidi wa wakati wetu wanahangaikia kwa kufikiria endapo ustaarabu utaendelea kuwepo, kwa sababu uhalifu unasonga mbele na kuonekana kuwa hauwezi kudhibitiwa.

I. Matetemeko ya ardhi yenye uharibifu, dhoruba, na njaa

**"Na kutakuwa na matetemeko makubwa ya nchi mahali mahali, na njaa na tauni." Luka 21:11 .**

Matetemeko ya ardhi, vimbunga, mafuriko, n.k. yanaongezeka kwa kasi isiyo na kifani. Theluthi moja ya watu wa dunia wana njaa, na maelfu wanakufa kila siku kwa njaa. Mambo hayo yote ni kithibitisho kwamba tunaishi katika saa za mwisho za dunia.

J. Ujumbe maalum kwa ulimwengu katika siku za mwisho kabisa

**"Injili hii ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja." Mathayo 24:14 .**

Ujumbe mkuu, mzito, wa mwisho wa onyo la ujio wa pili wa Kristo sasa unawasilishwa katika lugha na lahaja zaidi ya 900. Takriban asilimia 95 ya watu duniani wanapata ujumbe huu. Kabla ya kuja kwa Yesu mara ya pili, kila mtu ulimwenguni ataonywa kuhusu kurudi Kwake hivi karibuni. Watu watapotea ikiwa tu watakataa ujumbe wa huu onyo.

K. Kugeukia kuwasiliana na roho

**"Katika nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo." 1 Timotheo 4:1 . "Hao ni roho za mashetani." Ufunuo 16:14 .**

Watu wengi leo, ikiwemo idadi kubwa ya wakuu wa mataifa, hutafuta ushauri kutoka kwa wasomaji mikono, wachawi, na wapiga ramli. Kuwasiliana na mizimu ya watu waliokufa kale kumevamia makanisa, pamoja na fundisho la uongo la kutokufa kwa nafsi. Biblia inafundisha kwamba wafu wamekufa na hawana ufahamu wowote.

Tunaishi katika nyakati za mwisho.

**11. Ujio wa pili wa Bwana u karibu kiasi gani?**

"Basi jifunzeni mfano kwa mtini; tawi lake likiisha kuchipuka na kuchanua majani, mwajua ya kuwa wakati wa mavuno u karibu; Amin, nawaambia, Kizazi hiki

hakitapita, hata hayo yote yatimie. Mathayo 24:32-34 .

**Jibu:** Biblia ni mahususi sana na wazi juu ya jambo hili. Ishara karibu zote zimetimia. Hatuwezi kujua siku na saa kamili ya kurudi kwa Kristo ( Mathayo 24:36 ), lakini tunaweza kuwa na uhakika kwamba sisi ni watu ambao tutaishi kumwona Yesu akirudi. Mungu ameahidi kumaliza mambo haraka sana sasam na kuikata kazi yake na kuifupisha (Warumi 9:28 ). Kristo anarudi duniani kwa ajili ya watu Wake hivi karibuni. Je, Uko tayari?

Anayeonekana kuwa Yesu katika chumba cha mikutano ni mojawapo ya mapepo ya Shetani.

**12. Shetani anasema uwongo mwingi kuhusu ujio wa pili wa Kristo na, kwa maajabu na miujiza ya uongo, atawadanganya mamilioni. Ninawezaje kuwa na uhakika kwamba sitadanganywa?**

"Hao ni roho za mashetani, watendao miujiza." Ufunuo 16:14 .

"Nao watafanya ishara kubwa na maajabu wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule." Mathayo 24:24 .

"Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, ni kwa sababu hamna nuru ndani yao." Isaya 8:20 .

**Jibu:** Shetani amevumbua mafundisho mengi ya uwongo kuhusu ujio wa pili na anawadanganya mamilioni kuamini kwamba Kristo amekwisha kuja au kwamba atakuja kwa namna fulani isiyoandikwa kwenye Biblia. Lakini Kristo ametuonya juu ya mbinu ya Shetani, akisema, "Jihadharini mtu asiwadanganye." Mathayo 24:4 . Kisha anafichua mipango na uongo wa Shetani ili tupate kutahadharishwa, na anatukumbusha, "Tazama, nimekwisha kuwaambia." Mathayo 24:25 . Kwa mfano, Yesu alisema hasa kwamba hatatokea jangwani au kuja kwenye vyumba vya mikutano (mstari wa 26). Hakuna sababu ya kudanganywa ikiwa tunajifunza kile ambacho kitabu cha Mungu kinafundisha kuhusu kuja kwa pili kwa Kristo.

Kipimo cha mambo au waingereza wanasema kipimo cha acid/tindikali ni hiki: Biblia inafundisha nini kuhusu hili? Watu wanaojua Biblia inasema nini kuhusu ujio wa pili hawatapotoshwa na Shetani. Wengine wote watadanganywa ila wao hawatadanganywa.

Hatupaswi kuwa na shughuli nyingi hivi kwamba hatuna wakati wa kukaa na Kristo.

**13. Je, ninawezaje kuwa tayari wakati Yesu atakaporudi?**

"Yeye ajaye Kwangu sitamtupa nje kamwe." Yohana 6:37 .

"Wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu." Yohana 1:12.

"Nitatia sheria Zangu katika nia zao, na katika mioyo yao nitaziandika." Waebrania 8:10

“Ashukuriwe Mungu atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” 1 Wakorintho 15:57 .

**Jibu:** Yesu anasema, “Tazama, nasimama mlangoni [mlango huu unawakilisha akili au moyo wa mwanadamu], nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia.” Ufunuo 3:20 . Kupitia Roho Mtakatifu na dhamiri yangu, Yesu anabisha na kuomba aingie moyoni mwangu ili aweze kubadilisha maisha yangu. Nikimkabidhi maisha yangu bila kujibakiza, Yeye atafuta dhambi zangu zote za zamani ( Warumi 3:25 ) na kunipa uwezo wa kuishi maisha ya mbinguni ( Yohana 1:12 ). Kama zawadi ya bure, Yeye hunipa tabia Yake ya haki ili niweze kusimama bila woga mbele za Mungu mtakatifu maisha yangu yanapobadilishwa na Yesu. Ndipo kufanya mapenzi Yake inakuwa ni furaha kwangu. Jambo hilo ni rahisi sana hivi kwamba wengi wanatilia shaka Ukweli Wake. Lakini Hili ni Kweli. Sehemu yangu ya utendaji  ni kuyatoa maisha yangu kwa Kristo na kumwacha aishi ndani yangu. Sehemu Yake ni kufanya muujiza mkuu ndani yangu ambao unabadilisha maisha yangu na kunitayarisha kwa ujio Wake wa pili. Ni zawadi ya bure. Mimi nahitaji tu kuukubali mpango Wake, leo nikiisikia sauti Yake, sipaswi kuufanya moyo wangu kuwa mgumu.

**14. Kristo anaonya kwa uzito juu ya hatari gani kubwa?**

“Kwa hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa maana katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu Yuaja.” Mathayo 24:44 .

“Na jihadharini nafsi zenu isije ikalemewa na ulafi na ulevi na masumbufu ya maisha haya, siku hiyo ikawajieni ghafula. Luka 21:34 . “Lakini kama vile siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Mathayo 24:37 .

**Jibu:** Kuna hatari kubwa katika kujishughulisha sana na mahangaiko ya maisha haya au kuingiliwa na anasa za dhambi ili kuja kwa Bwana kuweze kutuchenga kama Gharika ilivyokuwa katika ulimwengu katika siku za Nuhu, nasi tutabaki kushangaa kwamba hatukujitayarisha, na kupotea. Hii itakuwa uzoefu wa mamilioni. Je, ni vipi kwako wewe, uko tayari? Yesu anarudi upesi sana—katika siku zetu hizi. Je, Unaweza kusema “Amina Uje Yesu”? Hakuna kitu kingine muhimu kuliko kujitayarisha kuishi milele na Bwana na kufurahia maisha ya mbinguni.

**15. Ninapanga kuwa tayari Yesu atakaporudi.**

**Jibu:**

## MASWALI YA KUFIKIRIA NA KUCHEUA

### 1. Je, ile dhiki kuu bado haijaja?

Ni kweli kwamba dhiki mbaya itafunika dunia kabla tu ya Yesu kurudi kuwakomboa watu Wake. Danieli anaufafanua huu muda kuwa ni "wakati wa taabu, ambao haujapata kuwapo kamwe." Danieli 12:1 . Ingawa hivyo, katika muktadha, "dhiki kuu" ya Mathayo 24:21 inarejelea mateso mabaya sana wa watu wa Mungu wakati wa Enzi za Giza. Mamilioni waliuawa kwa ajili ya imani yao wakati huo.

### 2. Kwa kuwa Bwana anakuja "kama mwivi usiku," mtu anawezaje kujua lolote juu Yake?

Jibu linapatikana katika 1 Wathesalonike 5:2-4 : "Kwa maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. kama vile utungu umpatavyo mwanamke mwenye mimba, wala hawataokoka. Lakini ninyi, ndugu, hamko gizani, hata siku hiyo iwapate kama mwivi." Angalia, siku ya Bwana inakuja kama mwivi kwa wasio tayari, lakini si kwa wale wanaoitwa "ndugu."

### 3. Kristo atasimamisha ufalme Wake duniani lini?

Baada ya kipindi kikuu cha miaka 1,000 cha Ufunuo 20. Kipindi cha miaka 1,000 huanza wakati wa ujio wa pili wa Kristo, wakati Yesu anachukua wenye haki kutoka duniani hadi mbinguni ili kuishi na kutawala pamoja Naye "miaka elfu." Ufunuo 20:4 . Mwishoni mwa ile miaka 1,000 "mji mtakatifu, Yerusalemu mpya" ( Ufunuo 21:2 ) utashuka kutoka mbinguni hadi duniani pamoja na watakatifu wote ( Zekaria 14:1 , 4 , 5 ) na waovu waliokufa katika nyakati zote watafufuliwa kwa uzima ( Ufunuo 20:5 ). Wanauzingira mji mtakatifu ili kuuteka ( Ufunuo 20:9 ), na moto unashuka kutoka kwa Mungu kutoka mbinguni na kuwateketeza. Moto huu unaitakasa dunia na kuteketeza athari zote za dhambi na wenye dhambi ( 2 Petro 3:10 ). Hatimaye moto unazimika ( Isaya 47:14 ), ukiacha majivu tu (Malaki 4:3 ). Kisha Mungu anaumba dunia mpya ( 2 Petro 3:13 ; Isaya 65:17 ;

Ufunuo 21:1 ) na kuwapa wenye haki, na kisha "Mungu ... atakaa nao, ... na Mungu Mwenyewe atakuwa pamoja nao, na kuwa Mungu wao." Ufunuo 21:3 . Viumbe wakamilifu, watakatifu, na wenye furaha, waliorudishwa tena kwenye sura kamilifu ya Mungu, hatimaye watakuwa nyumbani katika ulimwengu usio na dhambi, usio na doa kama vile Mungu alivyopanga awali. Ni mtu mpumbavu tu ndiye angechagua kukosa furaha hii ya milele.

### 4. Kwa nini hatusikii mahubiri na mafundisho zaidi leo kuhusu ujio wa pili wa Kristo?

Ibilisi anahusika na hili. Anajua vyema kwamba ujio wa pili ni "tumaini lenye baraka" ( Tito 2:13 ) la Mkristo, na pindi jambo hilo linapoeleweka, hubadilisha maisha ya wanaume na wanawake na kuwaongoza kufunga mkanda na kusimama dede kwa bidii na uhai katika kusambaza habari njema kwa wengine ili kuja Kwake Kristo kuharakishwe. Jambo h ilo humkasirisha Shetani, kwa hiyo huwavuta wale walio na "mfano wa utauwa" ( 2 Timotheo 3:5 ) lakini hukana "nguvu zake"

kudhihaki, wakisema, “Iko wapi ile ahadi ya kuja Kwake? , mambo yote yanaendelea kama yalivyokuwa tangu mwanzo.” 2 Petro 3:3 , 4 . Wale wanaokana, kupuuza, au kudharau ujio wa pili wa Kristo (kama tukio halisi, linalokuja hivi karibuni) wanatimiza kabisa unabii wa Biblia--na kumfanyia shetani huduma kuu sana.

**5. Lakini je, Yesu hakuwa akizungumza juu ya unyakuo wa siri aliposema katika Luka 17:36, “Mmoja atachukuliwa, na mwingine ataachwa”?**

Hapana hakusema hilo. Hakuna dalili hata kidogo kwamba tukio hilo la kuja kwa Yesu ni la siri. Yesu alikuwa anaelezea gharika ya Nuhu na uharibifu wa Sodoma. (Angalia Luka 17:26-37 .) Yesy Alisimulia jinsi Mungu alivyowaokoa Nuhu na Luti na kuwaangamiza waovu. Anasema hasa kwamba gharika na moto “ziliwaangamiza wote.” Mistari ya 27, 29. Kwa wazi, katika kila kisa, wachache walipelekwa mahali salama na wengine wakaangamizwa. Kisha akaongeza, “Ndivyo itakavyokuwa siku ile Mwana wa Adamu atakapofunuliwa.” Mstari wa 30. Kwa kielelezo, Yesu aliendelea, “Watu wawili watakuwa shambani, mmoja atatwaliwa, na mwingine ataachwa.” Aya 36. Hakuna siri juu yake. “Kila jicho litamwona.” Ufunuo 1:7 . Wakati wa kuja Kwake mara ya pili, Kristo ataonekana hadharani na waziwazi akiwachukua wenye haki juu mawinguni ( 1 Wathesalonike 4:16 , 17 ) na kuwaua waovu ( Isaya 11:4 ; 2 Wathesalonike 2:8 ). Ndiyo maana Luka 17:37 inazungumza juu ya miili ya waovu na inataja tai (au tai) waliokusanyika karibu nao. (Angalia pia Ufunuo 19:17, 18.) Waovu wanaoachwa nyuma wakati wa kuja kwa Kristo wanaachwa wakiwa wamekufa.

## MASWALI YA CHEMSHA BONGO, KWIZZ

**1. Wakati wa kuja Kwake mara ya pili (1)**
_____ Kristo atawasili faraghani na kutembelea miji fulani ya dunia.
_____ Kristo atatokea jangwani.
_____ Kristo atabaki mawinguni na kuwaita wenye haki juu ili wamlaki angani.

**2. Yesu atakaporudi katika dunia hii (1)**
_____ Wenye haki tu ndio watamwona.
_____ Kila jicho litamwona.
_____ Watu hawataijua hadi itangazwe kwenye TV.

**3. Nini kitatokea kwa wenye haki wakati wa kuja Kwake Krsito mara ya pili? (2)**
_____ Wafu wenye haki watafufuliwa, nao watapewa kutokufa, kisha watanyakuliwa juu katika mawingu, na kuchukuliwa mbinguni.
_____ Wenye haki watapewa kutokufa, watanyakuliwa juu katika mawingu, na kupelekwa mbinguni.
_____ Wenye haki watakaa hapa duniani na kuwaongoa waovu.
_____ Wenye haki watanyakuliwa kwa siri.

**4. Kwa mujibu wa ishara za Biblia, kuja kwa Kristo kuna uwezekano mkubwa wa kutokea (1)**

_____ Karibuni sana!
_____ Miaka mia kadhaa kutoka sasa.
_____ Katikati ya karne ya 21.

**5. Waovu ambao wanaishi wakati Yesu atakaporudi watawekwa (1)**
_____ Jehanamu, ambako wataungua milele.
_____ Watauawa wakati wa kuja Kwake mara ya pili.
_____ Watahifadhiwa na kupewa nafasi nyingine.

**6. Angalia kauli hapa chini zinazosema Ukweli kuhusu ujio wa pili wa Kristo: (4)**
_____ Atakuja kwa siri.
_____ Ujio wa pili ni uzoefu wa wongofu.
_____ Atakuja mawinguni.
_____ Kristo anakuja kwa ajili yetu saa ya kufa kwetu.
_____ Waovu hawatamwona.
_____ Malaika wote watakuwa pamoja Naye.
_____ Hataigusa au kuikanyaga dunia.
_____ Inawezekana kuijua siku na saa ya kuja Kwake.
_____ Mamilioni watashtuka/ watashangaa na kupotea.

**7. Wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili (1)**
_____ Ulimwengu wote utakuwa tayari na kusubiri.
_____ Kutakuwa na tetemeko la ardhi lenye kuangamiza ulimwenguni pote.
_____ Waovu wataongoka.

**8. Weka alama kwa kauli zote ambazo ni ishara za Kweli za siku za mwisho za dunia: (7)**
_____ Dunia itakuwa bora na bora zaidi.
_____ Mgogoro kati ya mtaji na kazi utatokea.
_____ Matetemeko machache ya ardhi, dhoruba, n.k.
_____ Kuanguka kutoka kwa Ukweli wa Biblia.
_____ Kiwango cha chini cha talaka.
_____ Wenda wazimu wa kujipatia anasa na raha.
_____ Kushuka kwa maadili.
_____ Kupungua kwa kiwango cha uhalifu.
_____ Njaa kubwa.
_____ Kuongezeka kwa maarifa.
_____ Machafuko na misukosuko.

**9. Ni ishara gani mbinguni ndizo ambazo ni ishara za kurudi kwa Kristo? (2)**
_____ Nyota ya Haley.
_____ Siku ya giza ya 1780.
_____ Nyota zilizoanguka Novemba 1833.
_____ Mwezi kuanguka duniani.

**10. Tunajuaje kwamba Yesu anarudi duniani hivi karibuni? (1)**
_____ Biblia inatoa ishara na maelezo kamili ya siku za mwisho.

_____ Kwa sababu watu wengi wanaamini kwamba Yesu anakuja upesi.
_____ Baadhi ya wabashiri wanatabiri.

**11. Mamilioni watadanganywa kuhusiana na namna na wakati wa kurudi kwa Kristo kwa sababu (1)**
_____ Mungu hataki wote waokolewe.
_____ Hawatoi matoleo ya sdaka makubwa vya kutosha.
_____ Hawasomi Biblia zao ili kupata Ukweli wa jambo hilo.

**12. Ninaweza kuwa tayari kwa kurudi kwa Kristo ikiwa (1)**
_____ Yesu anaishi ndani yangu.
_____ Ninasoma gazeti kila siku.
_____ Ninafanya kile ambacho Mchungaji au kasisi wangu anapendekeza

**Usafi wa moyo na Nguvu!**

**Somo la 9**

Je, umechoka kuwaumiza wapendwa wako na kuumiza dhamiri yako? Je, unaishi katika majuto ya mara kwa mara kwa makosa yako ya zamani? Umewahi kutamani kuoga na kuweza liwa msafi ndani na nje? Tuna habari njema kwako ... hakika unaweza! Mungu ana mpango ambao unaweza kuosha kabisa dhambi zako zote na kubadika tabia yako - hizi habari ni kweli au ni jambo ya kijinga tu? Hapana kabisa! Kristo anasema, “Tulizikwa pamoja Naye kwa ubatizo” ( Warumi 6:4 ). Unapomkubali Kristo, maisha ya kale yanakufa na Bwana anaahidi kusahau dhambi zetu zote! Si hivyo tu, Anaweza kukusaidia kushinda kila tabia ya dhambi maishani mwako. Je, unajua kwamba msalaba umetajwa mara 28 katika Biblia, lakini ubatizo umetajwa mara 97? Ni lazima jambo hili liwe la maana sana basi, na si ajabu, kwa sababu linaashiria maisha mapya kabisa na maisha ya zamani ya kuhuzunisha na ya dhambi yaliyozikwa na kusahaulika milele. Soma ukweli wa kushangaza wa Biblia juu ya somo hili la kushangaza ... hautakuwa kama ulivyo kamwe tena!

Mstari huu unaweka wazi kwamba ubatizo ni muhimu kwa wokovu.

**1. Je, ubatizo ni muhimu kweli?**

“Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.” Marko 16:16 .

**Jibu:** Ndiyo, kwa kweli! Lugha au maneno yoyote yangewezaje kuifanya iwe wazi zaidi?

Mazingira yalifanya kuwa jambo lisilowezekana kwa mwanadamu kwa mwizi pale msalabani kubatizwa.

**2. Lakini mwizi pale msalabani hakubatizwa, kwa nini nibatizwe basi?**

“Maana Yeye anatujua umbo letu, na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi.” Zaburi 103:14 .

**Jibu:** Wala hakurejesha alichokuwa ameiba, kama Bwana anavyoelekeza hasa katika Ezekieli 33:15 . Mungu anatuwajibisha kwa kile tunachoweza kufanya, lakini pia anatambua mipaka ya kwamba sisi tu "mavumbi." Naye Hatahitaji tufanye jambo lisilowezekana kimwili.

Je! Yule mwizi angeweza kushuka kutoka msalabani mara moja angebatizwa? Huu ndio mfano pekee katika Biblia ulio tofauti na kanuni hii. Mungu alitaka kuhakikisha kwamba hakuna mtu ambaye angekuwa na kimbelembele katika kukataa ubatizo.

Kuna Njia MOJA tu ya ubatizo ambayo ni ya kibiblia, sio 14.

**3. Kuna maagizo mengi yanayoitwa ubatizo. Je, Hakuna kati ya haya unaokubalika, mradi tu mtu ni mkweli na mwenye bidii kuhusu imani?**

"Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja." Waefeso 4:5 .

**Jibu:** Hapana! Kuna ubatizo mmoja tu wa Kweli. Ubatizo mwingine wote ni feki/bandia.

***Kumbuka:*** *Mpango wa " bafeti au kifurushi cha shetani" kwa ubatizo kinasema, "Chagua ubatizo unaotaka, kwani Mbinu ya ubatizo haijalishi". kinachojalisha ni moyo wako au roho yako inavyojisikia." Lakini Biblia inasema, "Bwana Mmoja, imani moja, ubatizo mmoja." Waefeso 4:5 . Pia Yeremia 38:20 inasema, "Nakusihi, uitii sauti ya Bwana."*

Yesu alibatizwa kwa kuzamishwa.

**4. Yesu alibatizwa jinsi gani?**

"Yesu ... akabatizwa na Yohana katika Yordani. Mara akipanda kutoka majini, aliona mbingu zimefunguka." Marko 1:9 , 10 .

**Jibu:** Kwa kuzamishwa kwenye maji! Angalia kwamba baada ya agizo hilo, alitoka "kutoka majini." Yesu alibatizwa "katika Yordani," si kwenye ukingo, kama wengi wanavyoamini. Yohana daima alikwenda mahali pa kubatiza watu ambapo "palikuwa na maji mengi" ( Yoh. 3:23 ), kwa hiyo pangekuwa na kina cha kutosha. Biblia inatuamuru kufuata mfano wa Yesu ( 1 Petro 2:21 ). Ubatizo wowote isipokuwa wa kuzamishwa unavunja amri hii. Neno "ubatizo" linatokana na neno la Kigiriki "baptizo." Ikimaanisha "kuzamisha chini au kuzamisha au kutumbukiza mwili mzima." Kuna maneno manane tofauti ya Kiyunani katika Agano Jipya yanayotumika kuelezea matumizi ya vimiminika. Lakini kati ya maneno haya mbalimbali--kama kunyunyiza, kumwaga, au kuzamisha--ni moja tu hapo lenye maana ya "kuzamisha" (baptizo) inatumiwa kuelezea ubatizo.

Filipo alimbatiza Mkushi au Muethiopia kwa kumzamishwa.

**5. Lakini je, wanafunzi au mitume hawakubadili njia ya ubatizo?**

"Wakashuka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza. Na walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo." Matendo 8:38, 39.

**Jibu:** Hapana! Tafadhali angalia kwamba Filipo, kiongozi katika kanisa la kwanza, alimbatiza mweka hazina wa Ethiopia kwa kuzamishwa sawasawa na vile

Yohana alivyokuwa akimbatiza Yesu. Na mtume Paulo alionya kwamba yeyote anayefundisha kinyume na yale ambayo Yesu alifundisha anapaswa “alaaniwe.” Wagalatia 1:8 . Hakuna mtu--hata kama mcha Mungu--aliyepewa mamlaka ya kubadilisha Maneno na Amri za Mungu.

Aina zote za ubatizo zisizokuwa za kuzamishwa hutoka kwa watu badala ya Maandiko.

**6. Kwa kuwa Yesu na wanafunzi walibatiza kwa kuzamishwa, ni nani aliyeanzisha haya mengine yanayoitwa ubatizo ambao upo leo?**

“Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.” Mathayo 15:9 .

**Jibu:** Wanaume waliopotoka walianzisha aina nyingine za ubatizo ambao unapingana moja kwa moja na Neno la Mungu. Yesu anasema, “Kwa nini ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?” “Hivi ndivyo mmeibatilisha amri ya Mungu kwa mapokeo yenu.” Mathayo 15:3 , 6 . Ibada inayofuata mafundisho ya wanadamu ni “batili.” Hebu fikiria! Ibada takatifu ya ubatizo imebadilishwa na kufanywa kuwa na athari kidogo wakati wa safari ya hatari ya Ukweli kwa karne nyingi. Si ajabu kwamba Biblia inatuhimiza “tushindane kwa bidii kwa ajili ya imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu. Yuda 3 .

Kuna mambo matatu rahisi ambayo mtu anapaswa kufanya kabla ya ubatizo.

**7. Mtu anapaswa kufanya nini ili kujitayarisha kwa ajili ya ubatizo?**

**Jibu:**

**A. Ajifunze matakwa ya Mungu.** “Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza ... na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi.” Mathayo 28:19 , 20 .

**B. Aamini Ukweli wa Neno la Mungu.**

“Aaminiye na kubatizwa ataokoka.” Marko 16:16 .

**C. Atubu na kuziacha dhambi zake na kuongoka.** “Tubuni, mkabatizwe kila mmoja kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi.” Matendo 2:38 . “Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe.” Matendo 3:19 .

Ninapobatizwa, ninathibitisha imani yangu katika kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu.

**8. Ni nini maana ya ubatizo?**

“Basi tulizikwa pamoja Naye kwa njia ya ubatizo katika mauti Yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. na kifo Chake sisi nasi tutakuwa katika mfano wa kufufuka Kwake; tukijua Neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja Naye, ili

mwili wa dhambi uharibiwe, tusitumikie dhambi tena. Warumi 6:4-6 .

**Jibu: U**nawakilisha mwamini anayemfuata Kristo katika kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka Kwake. Ishara ni kamilifu na imejaa maana ya kina. Katika ubatizo macho hufungwa, mikono inakunjwa, na pumzi inasimamishwa kana kwamba katika kifo. Kisha huja kuzikwa katika maji na ufufuo kutoka kaburi la maji hadi maisha mapya katika Kristo. Unapoinuliwa kutoka kwenye maji, macho hufunguka na anayebatizwa huanza kupumua tena na kuchanganyika na marafiki, mfano kamili wa ufufuo. Tofauti kubwa kati ya Ukristo na kila dini nyingine ni kifo, kuzikwa, na ufufuo wa Kristo. Katika matendo haya matatu, yale yote ambayo Mungu anatamani kutufanyia yanawezekana. Ili kuweka matendo haya matatu muhimu kuwa hai katika akili za Wakristo hadi mwisho wa wakati, Bwana alianzisha ubatizo wa kuzamishwa kama ukumbusho. Hakuna ishara ya kifo, kuzikwa, na ufufuo katika aina nyingine za ubatizo. Kule kuzamishwa tu kunatimiza maana ya Warumi 6:4-6.

Kufa kwa dhambi. Maisha ya zamani yaliyozikwa ndani ya maji. Na kuinuliwa au kufufuliwa kama mtu mpya katika Kristo.

Wakristo wapya ni kama watoto wachanga wanaojifunza kutembea. Wakati mwingine huteleza na kuanguka.

**9. Lakini mtu hapaswi kubatizwa hadi awe na uhakika kwamba hatateleza na kuanguka, au sivyo?**

"Kama kuna nia ya kutaka, inakubaliwa kama alivyo navyo mtu, si kama asivyo nacho. 2 Wakorintho 8:12 .

**Jibu:** Hii ni kama kusema mtoto hatakiwi kujaribu kutembea hadi ahakikishe kwamba hatateleza na kuanguka. Mkristo ni "mtoto" mchanga katika Kristo. Hii ndiyo sababu uzoefu wa uongofu unaitwa "kuzaliwa upya." Enzi mbaya na za dhambi hazipo tena kwa mtoto wa Mungu.

Dhambi ya mtu ya zamani husamehewa na kusahauliwa na Mungu, wakati wa kuongoka. Na ubatizo unaashiria kuzikwa kwa maisha hayo ya zamani. Tunaanza maisha ya Kikristo kama watoto wachanga, na si kama watu wazima, na Mungu hutuhukumu juu ya mtazamo wetu na mwelekeo wa maisha yetu, na si kuteleza na kujikwaa au kuanguka kidogo kunakotupata kama Wakristo wachanga.

Ubatizo ni tukio la utukufu kwa sababu unaashiria kuzikwa kwa maisha ya kale ya dhambi na mwanzo wa maisha mapya ndani ya Kristo.

**10. Kwa nini ubatizo ni jambo la dharura kwa mtenda-dhambi aliyeongoka?**

"Basi sasa unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia Jina la Bwana." Matendo 22:16 .

**Jibu:** Ubatizo ni ushuhuda wa hadharani kwamba mwenye dhambi aliyetubu amesamehewa na kusafishwa na Yesu (1 Yohana 1:9) na kwamba maisha yake ya zamani ya dhambi na ya usaliti yapo nyuma yake. Hakuna ushahidi wa hatia dhidi ya mtu baada ya wangofu.

Wanaume na wanawake leo wanayumba-yumba na kuhangaika chini ya mizigo mizito ya hatia na dhambi. Maambukizo na mzigo huu ni mbaya sana kwa utu wa mwanadamu, hivi kwamba watu watatataka wafanye lolote lile ili kufikia hisia ya msamaha na utakaso. Wengi wamesukumwa kwenye wodi la  magonjwa ya akili, ambapo wanadamu hujaribu kwa bidii kusaidia wanadamu wengine. Lakini msaada wa Kweli unapatikana katika kuja kwa Kristo, ambaye anawaambia wote wanaomkaribia, “Nataka takasika.” Mathayo 8:3 . Sio tu kwamba Yeye anasafisha, lakini pia anasulubisha asili ya zamani ya dhambi iliyo ndani yako. Kuzikwa katika maji ya ubatizo kunaashiria kuzikwa kwa maiti ya kutisha ya maisha ya zamani ya dhambi. Amri hiyo ni ya umuhimu mkubwa kwa sababu inawakilisha hadharani masharti ya ajabu sana kuwahi kutolewa kwa ajili ya watu.

Filipo alimbatiza mweka hazina Muethiopia/Mkushi siku ile ile alipomkubali Kristo kama Mwokozi wake.

**11. Inachukua muda gani kujitayarisha kwa ajili ya ubatizo?**

**Jibu:** Hiyo inategemea mtu. Wengine hushika vitu kwa haraka zaidi kuliko wengine. Lakini katika hali nyingi, maandalizi yanaweza kufanywa kwa muda mfupi. Hapa kuna baadhi ya mifano ya Biblia:

**A. Mweka hazina Muethiopia**

(Matendo 8:26-39) alibatizwa siku hiyohiyo aliposikia Ukweli.

**B. Mlinzi wa gereza wa Filipi na familia yake** ( Matendo 16:23-34 ) walibatizwa usiku huohuo waliposikia Ukweli.

**C. Sauli wa Tarso** ( Matendo 9:1-18 ) alibatizwa siku tatu baada ya Yesu kusema naye njiani kuelekea Damasko.

**D. Kornelio** ( Matendo 10:1-48 ) alibatizwa siku hiyohiyo aliposikia Ukweli.

**Katika uongofu, Mungu:**

1. Husamehe na kusahau yaliyopita.

2. Hutugeuza kimuujiza kuwa viumbe vipya vya kiroho.

3. Yeye Anatuchukua kama wana na binti Zake.

Kwa hakika hakuna mtu aliyeongoka Kweli ambaye angetaka kuchelewesha ubatizo, ambao unalipa hadharani sifa kwa Yesu kwa kufanya miujiza hii yote.

Mungu anapendezwa na watu wanaobatizwa kwa kuzamishwa. Je, Yesu anapendezwa na ubatizo wako?

**12. Mungu anahisije kuhusu ubatizo wa mtu aliyeongoka?**

**Jibu:** Alisema wakati wa ubatizo wa Mwanawe, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa Naye.” Mathayo 3:17 . Kwa hiyo, leo, Mungu hupendezwa sana

mtu anapobatizwa kwa kuzamishwa kupatana na amri Yake. Wale wanaompenda Bwana daima watajitahidi kumpendeza ( 1 Yohana 3:22 ; 1 Wathesalonike 4:1 ). Je, Mungu anapendezwa na ubatizo wako?

Ubatizo ni kuingia rasmi katika kanisa la Mungu. Kubatizwa bila kujiunga na kanisa la Mungu ni kinyume cha Biblia.

**13. Je, mtu anaweza kupata ubatizo wa Kweli bila kuwa mshiriki wa kanisa la Mungu?**

**Jibu:** Hapana! Mungu anaeleza jambo hili waziwazi. Zingatia hatua:

**A. Wote wameitwa katika mwili mmoja.** "Ninyi mmeitwa katika mwili mmoja." Wakolosai 3:15.

**B. Kanisa ni mwili.** "Yeye Ndiye kichwa cha mwili, cha kanisa." Wakolosai 1:18 .

**C. Tunaingia mwili huo kwa ubatizo.** "Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja." 1 Wakorintho 12:13 .

**D. Watu wa Mungu walioongoka huongezwa katika kanisa la Mungu.** "Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." Matendo 2:47 .

Ikiwa Yesu anazungumza nawe kuhusu ubatizo, usikahirishe. Ubatizo ni onyesho la hadharani la hamu yako ya kumfuata Mungu kikamilifu.

**14. Angalia mambo manne ambayo ubatizo haufanyi:**

**Jibu:**

**Kwanza**

Ubatizo wenyewe haubadilishi moyo wa mwanadamu bali ni ishara ya mabadiliko yaliyotokea. Mtu anaweza kubatizwa bila imani, bila toba, na bila moyo mpya. Anaweza hata kuzamishwa kwa kufuata mfano wa Yesu, lakini ataibuka kutoka kwenye maji kama mwenye dhambi aliyelowa badala ya mkavu, mtu asiye na imani, asiye na toba, asiye na moyo mpya. Ubatizo hauwezi kumfanya mtu mpya. Ubatizo hauwezi kubadilisha au kutengeneza upya mtu yeyote. Ni nguvu ya Roho Mtakatifu ndiyo inayobadilisha moyo katika wongofu. Ni lazima mtu azaliwe kwa Roho na vilevile azaliwe kwa maji.

**Cha Pili**

Sio lazima utamfanya mtu ajisikie vizuri. Sio lazima ubadilishe hisia zake. Baadhi ya watu wamekata tamaa kwa sababu hawajisikii tofauti baada ya kubatizwa. Wokovu si suala la hisia, bali ni imani na utii.

**Cha Tatu**

Ubatizo hauondoi majaribu. Ibilisi hajamalizana na mtu anapobatizwa. Lakini

Yesu Ndiye msaidizi wa kila muumini. Anasema, “Sitakupungukia kamwe, wala sitakuacha.” Waebrania 13:5 . Hakuna jaribu litakalokuja bila njia ya kuepuka. Hii ndiyo ahadi ya Maandiko Matakatifu ( 1 Wakorintho 10:13 ). Ubatizo

**Cha Nne**

Ubatizo hauhakikishi wokovu. Sio ibada ya kichawi (magic rite). Wokovu huja tu kama zawadi ya bure kutoka kwa Yesu Kristo wakati mtu anapitia kuzaliwa upya. Ubatizo ni ishara ya wongofu wa Kweli, na endapo wongofu hautatangulia ubatizo, sherehe hiyo haina maana.

**15. Yesu anakuomba ubatizwe kwa kuzamishwa kama ishara ya kwamba dhambi zako zimeoshwa. Je, ungependa kupanga kwa ajili ya agizo hili takatifu hivi karibuni?**

**Jibu:**

## MASWALI YA KUCHEUA NA KUFIKIRI

**1. Je, inafaa mtu kubatizwa zaidi ya mara moja?**

Ndiyo, Matendo 19:1-5 huonyesha kwamba Biblia inaunga mkono kubatizwa tena katika visa fulani.

**2. Je, watoto wachanga wabatizwe?**

Hapana! Hakuna anayepaswa kubatizwa isipokuwa (1) anaijua ile Kweli ya Mungu, (2) Anaiamini, (3) Ametubu, na (4) Ameongoka. Hakuna mtoto anayeweza kufuzu vigezo hivi hapa. Hakuna mtu aliye na haki ya kumbatiza mtoto. Kwa kweli, kufanya hivyo ni kupuuza kabisa amri za moja kwa moja za Mungu kuhusu ubatizo. Wanaume waliopotoshwa katika kanisa miaka iliyopita waliamuru kwamba watoto ambao hawajabatizwa wamepotea, lakini hii si kweli kimaandiko. Inakashifu tabia ya Mungu kwamba ni dhalimu asiye na haki ambaye angeangamiza watoto wachanga wasio na hatia waliokufa bila kubatizwa kwa sababu tu wazazi wasiojali wasiojua hawakuchukua hatua kufanya ubatizo wa watoto wao utendeke. Mafundisho kama haya ni ya kusikitisha kupita lugha ya kibinadamu. Ni mbaya vya kutosha kunyunyizia watoto wachanga maji na na kuuita ubatizo. Ni mbaya zaidi kushikilia dhana isiyo ya kimaandiko kwamba watoto wachanga wamepotea milele kwa sababu wazazi wazembe walishindwa kutimiza wajibu wao.

**3. Je, ubatizo si suala la maoni binafsi tu?**

Ndio, lakini sio maoni yako au yangu. Ni maoni ya Kristo ambayo ndiyo ya muhimu. Kristo anasema ubatizo ni muhimu Kwake. “Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.” Yohana 3:5 . Kukataa ubatizo ni kukataa ushauri wa moja kwa moja wa Mungu ( Luka 7:29 , 30 ).

**4. Mtu anapaswa kuwa na umri gani ili astahili kubatizwa?**

Mtu mzima vya kutosha kuelewa tofauti kati ya makosa na matendo au kutenda haki, na kufanya uamuzi wenye utashi katika kujisalimisha kwa Kristo na kumfuata. Watoto wengi wako tayari kwa ubatizo wakiwa na umri wa miaka 11 au 12, wengine wakiwa na miaka 7 au 8. Na wengine hawako tayari wakiwa na miaka 16 au 17. Hakuna kiwango cha umri kinachotajwa katika Biblia, kwa sababu watoto wana viwango tofauti vya uzoefu na uelewaji. Wengine wako tayari kwa ubatizo mapema kuliko wengine.

**5. Je, ubatizo peke yake unaweza kukuokoa?**

Hapana! Lakini kukataa kubatizwa kunaweza kusababisha mtu kupotea, kwa sababu inamaanisha kutotii. Wokovu ni kwa "wale wote wanaomtii". Waebrania 5:9 .

**6. Je, ubatizo wa Roho Mtakatifu si jambo la lazima?**

Hapana! Biblia inaonyesha katika Matendo 10:44-48 kwamba ubatizo wa maji ni muhimu, hata wakati ambapo ubatizo wa Roho Mtakatifu umetangulia.

**7. Je, hatupaswi kubatizwa kwa jJna la Yesu pekee?**

Katika Mathayo 28:19 , tunaambiwa tubatizwe katika jina la Baba, la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Hayo ni Maneno ya Yesu, na tunayaona kuwa ni matakatifu sana. Katika kitabu cha Matendo, tunapata waamini wapya waliobatizwa katika Jina la Yesu. Kumtambulisha Yesu kuwa Kristo na Masihi ilikuwa Kweli kwa watu wa siku hizo; kwa hiyo, ilikuwa muhimu kwao kubatizwa katika Jina Lake. Tunaamini ni muhimu sana kwetu leo pia. Tunapounganisha ushuhuda wa Mathayo na kitabu cha Matendo, tunabatiza watu katika Jina la Baba, na Mwana, Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu. Kufuata njia hii huzuia kuinua Andiko moja juu ya jingine.

**8. Kuna dhambi moja sitaki kuisalimisha. Je, nibatizwe?**

Hapana! Ni wazi kwamba hauko tayari kuzikwa katika maji ya ubatizo, kwa sababu maisha ya zamani ya dhambi hayajafa. Litakuwa ni tendo la uhalifu kwa msimamizi wa mazishi kumzika mtu ambaye hajafa na ni vibaya kwa mhudumu kumbatiza mtu ambaye maisha yake ya zamani ya dhambi hayajafa.

**9. Je, unaweza kueleza Wagalatia 3:27 ?**

Hapa Mungu analinganisha ubatizo na ndoa. Mtu anayebatizwa hivyo hukiri hadharani kwamba amechukua Jina la Kristo (Mkristo), kama vile bibi-arusi atangazavyo hadharani kuchukua jina la mume wake wakati wa arusi. Katika ubatizo, kama ilivyo kwa ndoa, sheria kadhaa hutumika kila wakati:

**A.** Haupaswi kamwe kuingizwa isipokuwa upendo wa Kweli utawale kuu.

**B.** Haupaswi kamwe kuingizwa isipokuwa mtahiniwa ameamua kuwa mwaminifu katika hali ngumu na nzuri.

**C. Uamuzi u**napaswa kufikiwa kwa ufahamu kamili.

**D.** Haupaswi kucheleweshwa isivyostahili.

## MASWALI YA CHEMSHA BONGO, KWIZZ

**1. Biblia inatuambia kwamba kuna Bwana mmoja, imani moja, na (1)**
_____ ubatizo 15.
_____ Ubatizo 5.
_____ 12 ubatizo.
_____ Ubatizo mmoja.

**2. Je, Yesu alifundisha umuhimu wa ubatizo? (1)**
_____ Ndiyo.
_____  Hapana.

**3. Yesu alibatizwa kwa (1)**
_____ Kumiminiwa maji.
_____ Kunyunyiziwa maji.
_____ Kuzamishwa majini.

**4. Neno "kubatiza" linamaanisha (1)**
_____ Kuwa na furaha.
_____ Kunyunyiziwa maji
_____ Kumiminiwa maji.
_____ Kuzamishwa chini au kutumbukizwa.

**5. Ubatizo mwingi wa uwongo wa siku hizi ulitolewa kwetu na (1)**
_____ Kristo.
_____ Mitume.
_____ Watu wapotofu.

**6. Weka alama kwenye mambo ambayo mtu anapaswa kufanya ili kujiandaa kwa ubatizo: (4)**
_____ Soma Biblia nzima mara tano.
_____ Amini Ukweli.
_____ Pata wongofu.
_____ Omba kwa siku 10 moja kwa moja.
_____ Tumia siku 40 kufunga.
_____ Jifunze matakwa ya Mungu.
________ Tubu na uache dhambi.

**7. Ubatizo ni ishara ya (1)**
_____ Kuumbwa kwa ulimwengu.
_____  Biblia.
_____ Mbingu.
_____ Kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Kristo.
_____ Malaika.

**8. Mkristo aliyebatizwa hivi karibuni ni (1)**
_____ mtoto wa kiroho.
_____ Mtu mzima wa kiroho.

**9. Ubatizo unapoingiwa kwa maombi, unyofu, na ufahamu (1)**
_____ Hukiri au hushuhudia wongofu mbele ya watu.
_____ Humaanisha zaidi ya kuogelea.
_____ Humhakikishia mtu hatajaribiwa tena.

**10. Je, ubatizo wa watoto wachanga unatoka kwenye Maandiko? (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**11. Watoto wengine wako tayari kwa ubatizo mapema zaidi kuliko wengine. (1)**
_____ Kweli.
_____ Uongo.

**12. Je, mtu ni lazima achukue majuma au miezi mingi ili kujitayarisha kwa ajili ya ubatizo? (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**13. Je, mtu anaweza kupata ubatizo wa kweli bila kuwa mshiriki wa kanisa? (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

## Je, Ni Kweli Wafu Wamekufa?

### Somo la 10

Kifo kinaweza kuwa mojawapo ya mambo yasiyoeleweka sana leo. Kwa wengi kimegubikwa na fumbo na kinaibua hisia za kutisha za woga, kutokuwa na uhakika, na hata kukosa tumaini. Wengine wanaamini kwamba wapendwa wao waliokufa hawajafa kabisa, bali wanaishi nao au wapo katika maeneo mengine! Wengine huamini kwamba wapendwa wao wanazaliwa mahali pengine duniani kama watu wenye vyeo vya juu au wanyama kutegemea na wema walioufanya kabla ya kufa. Bado wengine wamechanganyikiwa kuhusu uhusiano kati ya mwili, roho, na nafsi. Lakini je, inajalisha wewe unachoamini? Ndiyo... kabisa! Kwa sababu yale unayoamini kuhusu wafu yatakuwa na matokeo makubwa juu ya yale yatayokupata katika nyakati za mwisho. Hatuna nafasi ya kubahatisha, kwa hivyo Mwongozo huu wa Mafunzo utakupa kile hasa ambacho Mungu anasema kuhusu somo hili. Jitayarishe kwa kupata hichi kifungua macho halisi!

Adamu aliumbwa na Mungu hapo mwanzo.

**1. Tumefikaje hapa duniani kwanza?**

“Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.” Mwanzo 2:7 .

**Jibu:** Mungu alituumba kwa udongo hapo mwanzo.

Roho za wote wenye haki na waovu hurudi kwa Mungu. Miili yao hurudi mavumbini.

**2. Ni nini hutokea mtu anapokufa?**

“Ndipo mavumbi yatairudia ardhi kama yalivyokuwa; na roho itarudi kwa Mungu aliyeitoa.” Mhubiri 12:7 .

**Jibu:** Mwili unageuka kuwa mavumbi tena, na roho inarudi kwa Mungu, aliyeitoa. Roho ya kila mtu anayekufa—awe mwadilifu au mwovu—humrudia Mungu anapokufa.

Hakuna jambo la ajabu kuhusu roho ambayo inamrudia Mungu anapokufa. Hii Ni pumzi ya uhai.

**3. Ni nini “roho” inayomrudia Mungu wakati wa kifo?**

“Mwili bila roho [“pumzi,” tazama pambizo] umekufa.” Yakobo 2:26 . “Roho ya Mungu [“pumzi ambayo Mungu alimpa,” tazama pambizo] i katika pua yangu.” Ayubu 27:3 .

**Jibu:** Roho inayomrudia Mungu wakati wa kifo ni pumzi ya uhai. Hakuna mahali popote katika kitabu chote cha Mungu ambapo “roho” ina uhai, hekima, au hisia baada ya mtu kufa. Roho ni “pumzi ya uzima” na hakuna zaidi ya hilo.

Watu hawa wanne ni nafsi nne.

**4. “Nafsi” ni nini?**

“Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.” Mwanzo 2:7 .

**Jibu:** Nafsi ni kiumbe hai. Nafsi daima ni mchanganyiko wa vitu viwili: *mwili pamoja na pumzi* . Nafsi haiwezi kuwepo isipokuwa mwili na pumzi vimeunganishwa. Neno la Mungu linafundisha kwamba sisi ni nafsi.

**5. Je, nafsi hufa?**

“Roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa.” Ezekieli 18:20 . “Kila nafsi hai ilikufa baharini.” Ufunuo 16:3 .

**Jibu:** Kulingana na Neno la Mungu, nafsi hufa! Sisi ni nafsi, na nafsi hufa. Mwanadamu anakufa ( Ayubu 4:17 ). Mungu pekee Ndiye asiyeweza kufa ( 1 Timotheo 6:15 , 16 ). Dhana ya nafsi isiyoweza kufa na isiyoweza kufa inapingana na Biblia, ambayo inafundisha kwamba nafsi zinaweza kufa.

**6. Je, watu wema huenda mbinguni wanapokufa?**

“Wote waliomo makaburini wataisikia sauti Yake, Nao watatoka.” Yohana 5:28 , 29 . “Daudi ... amekufa akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo.” “Kwa maana Daudi hakupanda mbinguni.” Matendo 2:29 , 34 . “Nikingoja, kaburi ni nyumba yangu.” Ayubu 17:13 .

**Jibu:** Hapana, watu hawaendi mbinguni au motoni wanapokufa. Wanaenda kwenye makaburi yao kusubiri siku ya ufufuo.

**7. Ni kiasi gani mtu anajua au kuelewa baada ya kifo?**

“Walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Tena upendo wao, na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote; hawana sehemu tena milele katika jambo lo lote linalofanyika chini ya jua. “Hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, kuzimu uendako wewe.” Mhubiri 9:5 , 6 , 10 . “Wafu hawamsifu Bwana.” Zaburi 115:17 .

**Jibu:** Mungu anasema kwamba wafu hawajui lolote kabisa!

Ingawa mamilioni wanafikiri inawezekana, wafu hawawezi kuwasiliana na walio hai.

**8. Lakini je, wafu hawawezi kuwasiliana na walio hai, na je, hawajui wanalofanya walio hai?**

“Ndivyo mwanadamu hulala chini, asiinuke; “Wanawe hufikilia heshima, wala yeye hajui; Kisha wao huaibishwa, lakini yeye hana habari zao.” Ayubu 14:12 , 21. “Wala hawana sehemu tena milele katika jambo lolote linalofanyika chini ya jua.” Mhubiri 9:6 .

**Jibu:** Hapana, wafu hawawezi kuwasiliana na wale walio hai, wala hawajui wanachofanya walio hai. Wamekufa. Mawazo yao yamepotea ( Zaburi 146:4 ).

Yesu anakiita kifo “usingizi”. Ni hali ya kupoteza fahamu kabisa.

**9. Yesu aliita hali ya kutofahamu ya wafu “usingizi” katika Yohana 11:11-14. Watalala mpaka lini?**

“Ndivyo mwanadamu hulala chini, asiinuke; Ayubu 14:12 .

“Siku ya Bwana itakuja ... ambayo mbingu zitapita.” 2 Petro 3:10 .

**Jibu:** Wafu watalala mpaka siku kuu ya Bwana kwenye mwisho wa dunia. Katika kifo, wanadamu hawana fahamu kabisa bila shughuli au ujuzi wa aina yoyote.

Wenye haki watafufuliwa na kupewa kutokufa katika ujio wa pili wa Yesu.

**10. Ni nini kinatokea kwa wafu wenye haki katika ujio wa pili wa Kristo?**

"Tazama, Naja upesi, na ujira wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo." Ufunuo 22:12 . "Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, ... na waliokufa katika Kristo watafufuliwa ... na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele." 1 Wathesalonike 4:16 , 17 . "Sisi sote tutabadilishwa, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, ... na wafu watafufuliwa wasiwe na uharibifu.... Maana lazima huu uharibikao uvae kutokuharibika, na huu wa kufa uvae kutokufa." 1 Wakorintho 15:51-53 .

**Jibu:** Watalipwa. Watafufuliwa, watapewa miili isiyoweza kufa, na kunyakuliwa ili kumlaki Bwana hewani. Hakungekuwa na kusudi la ufufuo ikiwa watu wangepelekwa mbinguni wanapokufa. Kwanini makaburi yafunuke na wafu watoke, wakati wapo mbinguni tayari?

Uongo wa kwanza wa shetani kwa Hawa ulikuwa "Hamtakufa" - kauli iliyo kinyume kabisa na Maandiko yote.

**11. Uongo wa kwanza wa shetani ulikuwa upi?**

"Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa." Mwanzo 3:4 . "Yule nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi, na Shetani." Ufunuo 12:9 .

**Jibu:** Shetani alimwambia Hawa kwamba dhambi haitaleta kifo. "Hakika hamtakufa," akasema.

Wale wanaoamini kuwa wafu wako hai huwa walengwa rahisi wa udanganyifu wa shetani.

**12. Kwa nini Ibilisi alimdanganya Hawa kuhusu kifo? Je, somo hili linaweza kuwa muhimu zaidi kuliko wengi wanavyofikiri?**

**Jibu:** Ni moja ya nguzo za ufalme wa shetani. Amefanya miujiza yenye nguvu tangu zamani zote kupitia watu wanaodai kupokea nguvu zao kutoka kwa roho za wafu. (Mifano: Wachawi wa Misri Kutoka 7:11 , Mwanamke wa Endori 1 Samweli 28:3-25 , Wachawi katika Danieli 2:2 , Msichana fulani mwenye nguvu za uaguzi Matendo 16:16-18 .)

**Onyo Zito**

Katika wakati wa mwisho Shetani atafanya tena. Atatumia uchawi kama alivyofanya katika siku za Danieli kudanganya ulimwengu ( Ufunuo 18:23 ). Uchawi ni wakala usio wa kawaida (supernatural) unaodai kupokea nguvu na hekima yake kutoka kwa roho za wafu.

**Kujifanya Kama Wanafunzi wa Yesu**

Wakijifanya kuwa ni wapendwa waliokuwa waumini ambao wamekufa, makasisi watakatifu ambao walikufa zamani, manabii wa Biblia wa zamani, au hata mitume au wanafunzi wa Kristo (2Wakorintho 11:13 ), Shetani na malaika zake

watadanganya mabilioni ya watu. Wale wanaoamini kwamba wafu wako hai, kwa namna yoyote ile, bila shaka watadanganyika.

Miujiza yote haitoki kwa Mungu, kwa sababu mashetani pia hufanya miujiza.

**13. Je, ni kweli mashetani hufanya miujiza?**

"Hao ni roho za mashetani, watendao miujiza." Ufunuo 16:14 . "Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule." Mathayo 24:24 .

**Jibu:** Ndiyo, kwa kweli Mashetani hufanya miujiza yenye kusadikisha sana ( Ufunuo 13:13, 14). Shetani na malaika zake watatokea kama malaika wa nuru (2 Wakorintho 11:14 ) na, hata kwa kushangaza watu zaidi, watafanya maigizo kwamba wao ndio Kristo Mwenyewe ( Mathayo 24:23 , 24 ). Hisia za ulimwengu mzima zitakuwa kwamba Kristo na malaika zake wanaongoza nje katika uamsho wa ajabu duniani kote. Msisitizo mzima utaonekana kuwa wa kiroho sana na kuwa wa ajabu sana hivi kwamba ni wateule wa Mungu pekee ambao hawatadanganywa.

Wateule hawatadanganywa, kwa sababu wanakataa kabisa kila kitu ambacho ni kinyume na Maandiko.

**14. Kwa nini watu wa Mungu hawatadanganywa?**

"Walipokea lile Neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kama mambo hayo ndivyo yalivyo." Matendo 17:11 . "Ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, ni kwa sababu hamna nuru ndani yao." Isaya 8:20 .

**Jibu:** Watu wa Mungu watajua kutokana na funzo lao la bidii la kitabu Chake kwamba wafu wamekufa,  si hai. Roho za wafu hazipo. Kwa hiyo, watu wa Mungu watakataa watenda miujiza na walimu wote wanaodai kupokea "nuru" ya pekee au kufanya miujiza kwa kuwasiliana na roho za wafu. Na watu wa Mungu pia watakataa mafundisho yote hatari na ya uongo yanayodai kwamba wafu wako hai kwa namna yoyote, popote.

Katika siku za Musa, watu waliodai kuwa na uwezo wa kuwasiliana na wafu walipigwa mawe hadi kufa.

**15. Huko nyuma katika siku za Musa, Mungu aliamuru nini kifanyike kwa watu waliofundisha kwamba wafu walikuwa hai?**

"Tena mtu mume au mke aliye na pepo, au aliye mchawi, hakika atauawa; watampiga kwa mawe." Mambo ya Walawi 20:27 .

**Jibu:** Mungu alisisitiza kwamba wachawi na wengine wenye "roho za utambuzi" (waliodai kuwa na uwezo wa kuwasiliana na wafu) wanapaswa kupigwa mawe hadi kufa. Hilo linaonyesha jinsi Mungu anavyoona fundisho la uongo kwamba wafu wako hai.

Hakuna mtu katika ufalme mpya wa Mungu atakayekufa milele. Kifo kitakoma wakati Shetani atakapoangamizwa.

**16. Je, watu waadilifu watakaofufuliwa katika ufufuo watakufa tena?**

“Wale watakaohesabiwa kuwa wamestahili kuupata ulimwengu ule, na kufufuka katika wafu, ... wala hawawezi kufa tena.” Luka 20:35 , 36 . “Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.” Ufunuo 21:4 .

**Jibu:** Hapana! Kifo, huzuni, kilio, na misiba havitaingia kamwe katika ufalme mpya wa Mungu.

Kuzaliwa upya haiwezekani. Kwa sababu Mungu anasema wote waliokufa, wema na waovu, wako makaburini mwao.

**17. Imani katika kuzaliwa upya katika umbo jingine inaendelea kukua kwa haraka sana leo. Je, mafundisho haya ni ya kibiblia?**

“Walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote. ... wala hawana sehemu tena katika jambo lo lote linalofanyika chini ya jua milele.” Mhubiri 9:5 , 6.

**Jibu:** Karibu nusu ya watu duniani wanaamini katika kuzaliwa upya katika umbo jingine, fundisho la kwamba nafsi haifi kamwe bali huendelea kuzaliwa upya katika aina tofauti ya mwili na kila kizazi kinachofuata. Mafundisho haya, hata hivyo, ni kinyume na Maandiko.

**Biblia Inasema**

Baada ya kifo mtu: hurudi mavumbini ( Zaburi 104:29 ), hajui lolote ( Mhubiri 9:5 ), hana nguvu za kiakili ( Zaburi 146:4 ), hana uhusiano wowote na kitu chochote duniani ( Mhubiri 9:10; 6 ), haishi ( 2 Wafalme 20:1 ), anangoja kaburini ( Ayubu 17:13 ), na haendelei ( Ayubu 14:1 , 2 ).

**Uvumbuzi wa Shetani**

Tulijifunza katika swali la 11 na 12 kwamba Shetani ndiye aliyebuni fundisho la kwamba wafu wako hai. Kuzaliwa upya katika mwili baada ya kufa mahali pengine duniani (reincarnation kama wanavyoamini dini ya Hindu), uchawi, kuwasiliana na roho zilizokufa, ibada ya mizimu, na “nafsi isiyokufa” yote ni uvumbuzi au ubunifu wa Shetani, kwa lengo moja la kuwasadikisha watu kwamba unapokufa hujafa kwelikweli. Watu wanapoamini kwamba wafu wako hai, “roho za mashetani, wanaofanya miujiza” ( Ufunuo 16:14 ) na kujifanya kuwa roho za wafu wataweza kuwadanganya na kuwapotosha karibu asilimia 100 ya watu wakati huo ( Mathayo 24:24 ) )

Wale wanaosisitiza juu ya uthibitisho wa Maandiko kwa mafundisho yote hawatapotoshwa na Shetani.

**18. Ninashukuru kwa ajili ya Biblia, ambayo hutuambia Ukweli juu ya suala hili nyeti la kifo.**

**Jibu:**

## MASWALI YA KUFIKIRIA NA KUCHEUA

**1. Je, mwizi pale msalabani hakwenda paradiso pamoja na Kristo siku alipokufa?**

Hapana. Kwa kweli, Jumapili asubuhi Yesu alimwambia Mariamu, "Sijapaa kwenda kwa Baba Yangu." Yohana 20:17 . Hilo linaonyesha kwamba Kristo hakwenda mbinguni alipokufa. Pia kumbuka kuwa alama za uakifishaji (koma, nukta nk) katika Biblia hazijavuviwa, bali ziliongezwa na wanadamu. Ile Koma katika Luka 23:43 inapaswa kuwekwa baada ya maneno "leo" na siyo kabla, hivyo fungu hili linasomeka, "Amin, nakuambia leo, utakuwa pamoja Nami katika paradiso." Au, "Ninakuambia hivi leo - wakati inaonekana kwamba Mimi siwezi kumwokoa mtu yeyote, wakati Mimi Mwenyewe ninasulubishwa kama mhalifu - nakuambia hivi leo kwamba utakuwa pamoja Nami katika paradiso." Ufalme wa Kristo utasimikwa wakati wa kuja Kwake mara ya pili (Mathayo 25:31 ), na wenye haki wote wa nyakati zote watauingia ufalme wakati huo ( 1 Wathesalonike 4:15-17 ) na si kifo.

**2. Je, Biblia haisemi juu ya nafsi "isiyokufa," "roho isiyokufa"?**

La, nafsi isiyoweza kufa haitajwi katika Biblia. Neno "kutoweza kufa au kutokufa" linapatikana mara moja tu katika Biblia, na linarejelea Mungu ( 1 Timotheo 1:17 ).

**3. Wakati wa kufa mwili hurudi mavumbini na roho (au pumzi) inamrudia Mungu. Lakini roho huenda wapi?**

Haiendi popote. Badala yake, inakoma tu kuwepo. Vitu viwili lazima viunganishwe ili kuunda roho: *mwili na pumzi* . Pumzi inapotoka, roho huacha kuwapo kwa sababu ni mchanganyiko wa vitu viwili. Unapozima taa, mwanga huenda wapi? Hauendi popote. Unakoma tu kuwepo. Mambo mawili lazima yaunganishwe ili kutengeneza mwanga: *balbu na umeme*. Bila mchanganyiko wa hayo mawili, mwanga hauwezekani kuwepo. Hivyo kwa nafsi; isipokuwa na mwili na pumzi vikaunganishwa pamoja, hakuwezi kuwa na roho. Hakuna kitu kama roho isiyo na mwili.

**4. Je, neno "nafsi" huwa na maana nyingine yoyote isipokuwa kiumbe hai?**

Ndiyo, inaweza kumaanisha pia (1) maisha yenyewe, au (2) akili, au utashi. Haidhuru ni maana gani inayokusudiwa, nafsi ingali ni muunganiko wa vitu viwili (mwili na pumzi), nayo hukoma kuwepo wakati wa kufa.

**5. Je, unaweza kueleza Yohana 11:26 , inayosema, "Na kila aishiye na kuniamini hatakufa hata milele"?**

Hii hairejelei kifo cha kwanza, ambacho watu wote hufa ( Waebrania 9:27 ), lakini kifo cha pili, ambacho ni waovu tu hufa na ambacho hakuna ufufuo ( Ufunuo 2:11 ; 21:8 ).

**6. Mathayo 10:28 inasema, "Msiwaogope wauao mwili, lakini hawawezi kuiua roho." Je, hii haithibitishi kwamba nafsi haifi?**

Hapana, inathibitisha kinyume chake. Nusu ya mwisho wa aya hiyo hiyo inathibitisha kwamba nafsi hufa. Inasema, "Lakini afadhali mwogopeni Yule awezaye *kuangamiza mwili na roho pia katika jehanum* ." Neno "nafsi" hapa linamaanisha uzima na linamaanisha uzima wa milele, ambao ni zawadi ( Warumi 6:23 ) ambao utatolewa kwa wenye haki siku ya mwisho ( Yohana 6:54 ). Hakuna anayeweza kuchukua uzima wa milele ambao Mungu hutoa. (Angalia pia Luka 12:4 , 5 .)

**7. Je, 1 Petro 4:6 haisemi injili ilihubiriwa kwa watu waliokufa?**

Hapana, inasema injili "ilihubiriwa" kwa wale "waliokufa". Wamekufa sasa, lakini injili "ilihubiriwa" walipokuwa bado hai.

**8. Je ni nini kinachoendelea kuhusu nafsi zinazolia kutoka chini ya madhabahu katika Ufunuo 6:9, 10 ? Je, hili halionyeshi kwamba nafsi hazifi?**

Hapana. Kilio hiki kilikuwa cha mfano, kama vile kilio cha damu ya Abeli ( Mwanzo 4:10 ). Neno "nafsi" hapa linamaanisha watu (au viumbe hai) ambao walikuwa wameuawa kwa ajili ya imani yao. Kwa hakika hakuna anayeamini kwamba nafsi zinazokufa hulala kihalisi chini ya madhabahu, wala watu hawaamini kwamba wenye haki humwomba Mungu awaadhibu adui zao. Badala yake, wenye haki huomba rehema kwa adui zao, kama Kristo alivyofanya msalabani ( Luka 23:34 ).

**9. Je, Biblia haisemi Kristo alienda na kuwahubiria roho zilizopotea kuzimu kati ya kusulubishwa Kwake na ufufuo?**

Hapana, andiko la Biblia linalozungumziwa ni 1 Petro 3:18-20 . Mahubiri yalifanywa "kwa Roho" (mstari 18) katika siku za Nuhu—kwa watu waliokuwa wakiishi wakati huo (mistari 19, 20). "Roho zilizofungwa" inarejelea watu ambao maisha yao yalikuwa katika utumwa wa Shetani. (Angalia Zaburi 142:7 ; Isaya 42:6 , 7 ; 61:1 ; na Luka 4:18 .)

## <u>MASWALI YA CHEMSHA BONGO KWIZZ</u>

**1. Biblia inazungumza juu ya kifo kama (1)**

_____ Usingizi.
_____ Mabadiliko ya aina tofauti ya maisha.
_____ Siri isiyoelezeka.

**2. "Roho" inayomrudia Mungu wakati wa kifo ni (1)**

_____ Utu halisi wa ndani wa mtu.
_____ Roho.
_____ Pumzi ya uhai.

**3. Mtu akifa huenda (1)**
_____ Mbinguni au kuzimu.
_____ Kaburini.
_____ Toharani.

**4. Nafsi ni (1)**
_____ Asili ya kiroho ya mtu.
_____ Sehemu isiyoisha ya mtu.
_____ Kiumbe hai.

**5. Je, nafsi hufa? (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**6. Waadilifu wanathawabishwa lini? (1)**
_____ Katika maisha haya.
_____ Wakati wa kifo.
_____ Katika ujio wa pili wa Kristo.

**7. Kwa nini Shetani anajaribu kuwadanganya watu kwa kuwaambia wafu hawajafa? (1)**
_____ Ili waamini miujiza yake na kudanganyika na kupotea.
_____ Kwa sababu anawahurumia.
_____ Kwa sababu yeye ni mkatili na mwovu.

**8. Watu ambao "wanawasiliana" na wafu wanazungumza na (1)**
_____ Roho zisizokufa.
_____ Malaika watakatifu.
_____ Pepo wachafu wanaomwiga marehemu.

**9. Katika siku za Musa Mungu aliamuru kwamba wote waliofundisha kwamba wafu wako hai wawe (1)**
_____ Wafanywe makuhani.
_____ Waheshimiwe kwa hekima zao.
_____ Wauwawe.

**10. Mtu anawezaje kuwa na uhakika kwamba yuko salama na yuko sawa? (1)**
_____ Mwombe Mungu ishara maalum kutoka mbinguni.
_____ Fanya kile mchungaji au mhubiri anasema kufanya.
_____ Jifunze Biblia kwa maombi na kwa uangalifu na uifuate.

**11. Mtu anapokufa (1)**
_____ Roho, au nafsi yake, hubaki hai.
_____ Ana uwezo wa kutazama walio hai na kuwasiliana nao.
_____ Amekufa kwa kila njia--mwili hufa, roho hukoma kuwapo, na hakuna

uwezekano wa mawasiliano na wale walio hai.

**12. Je, miujiza ni uthibitisho wa kwamba jambo hilo ni la Mungu? (1)**
_____ Ndiyo. Ni Mungu pekee awezaye kufanya miujiza.
_____ Hapana. Ibilisi pia atafanya miujiza mikubwa.

## Je, Ibilisi Ndiye bosi anayesimamia Kuzimu/Jehanamu?

### Somo la 11

Wacha tuangalie zaidi kwa undani. Je! ni kweli Mungu humweka shetani kwenye orodha yake ya wapokea mshahara - je, yeye ndiye msimamizi mkuu wa kuzimu anayepima adhabu ya waliopotea? Takriban ulimwengu mzima una maoni yasiyo ya kibiblia kuhusu kuzimu, na una deni kwako mwenyewe kujua kile ambacho Biblia inasema kuhusu Jehanamu. Usidanganywe, kwa sababu kile unachofikiri kuhusu Jehanamu hakika huathiri kile unachofikiri kuhusu tabia ya Mungu! Chukua muda mfupi kupata mambo ya ajabu unayohitaji kujua leo!
Waovu hawataadhibiwa mpaka baada ya hukumu.

**1. Ni roho ngapi zilizopotea zinazoadhibiwa kuzimu leo?**

"Bwana ajua kuwaokoa watauwa na majaribu, na kuwaweka wasio haki katika majaribu hata siku ya hukumu." 2 Petro 2:9 .

**Jibu:** Hakuna hata nafsi moja iliyo katika moto wa Jehanamu leo. Biblia inasema kwamba Mungu huwahifadhi, au huwazuia waovu mpaka siku ya hukumu waadhibiwe.

Wenye dhambi watatupwa jehanamu yenye moto mwisho wa dunia -- si watakapokufa.

**2. Ni wakati gani wenye dhambi watatupwa katika moto wa mateso?**

"Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia hii. Mwana wa Adamu atawatuma malaika Zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme Wake machukizo yote, na watenda maovu, na kuwatupa katika tanuru ya moto. ." Mathayo 13:40-42 . "Neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho." Yohana 12:48 .

**Jibu:** Wenye dhambi watatupwa katika moto wa Jehanamu katika siku kuu ya hukumu mwishoni mwa ulimwengu—si watakapokufa. Mungu asingemwadhibu mtu kwa moto hadi kesi yake isikilizwe na kuamuliwa mahakamani mwishoni mwa ulimwengu. Wala Mungu asingeteketeza muuaji aliyekufa miaka 5,000 iliyopita, miaka 5,000 zaidi ya yule anayekufa na anayestahili adhabu kwa dhambi hiyo hiyo leo.

Wote waliokufa, wema na waovu, wako makaburini wakingojea ufufuo.

**3. Wako wapi wenye dhambi (waliokufa) sasa?**

"Saa yaja ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti Yake, nao watatoka, wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu. " Yohana 5:28 , 29 . "Waovu huhifadhiwa hadi siku ya uharibifu." "Lakini atapelekwa kaburini, na kukaa kaburini." Ayubu 21:30 , 32 .

**Jibu:** Biblia ni maalum/mahususi. Waovu na waadilifu ambao wamekufa wote wako makaburini mwao "wamelala" hadi siku ya ufufuo.

Yesu alikufa ili kutuokoa na dhambi zetu. Wale wasiokubali zawadi Yake ya wokovu watapokea kifo.

**4. Matokeo ya mwisho ya dhambi ni nini?**

"Mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu." Warumi 6:23 . "Dhambi, ikiisha kukoma, huzaa mauti." Yakobo 1:15 . "Mungu ... alimtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16 .

**Jibu:** Mshahara (au adhabu) kwa ajili ya dhambi ni kifo, si uzima wa milele katika moto wa mateso. Waovu "wanaangamia," au kupokea "kifo." Wenye haki wanapokea "uzima wa milele."

Waovu hawafi. Biblia inasema "wataangamia", "watateketezwa" na "kuangamizwa".

**5. Ni nini kitakachowapata waovu katika moto wa mateso?**

"Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti; hiyo ndiyo mauti ya pili." Ufunuo 21:8 .

**Jibu:** Waovu hufa kifo cha pili katika moto wa Jahanamu. Ikiwa waovu wangeishi milele wakiteswa motoni, wangekuwa wenye kutokufa, au wasioweza kufa au wenye uzima wa milele! Lakini hilo haliwezekani, kwa sababu Biblia inasema Mungu "pekee Ndiye asiyeweza kufa." 1 Timotheo 6:16 . Adamu na Hawa walipofukuzwa kutoka katika bustani ya Edeni, malaika aliwekwa ili kuulinda mti wa uzima ili wenye dhambi wasile matunda ya mti huo na "kuishi milele kwa huzuni." Mwanzo 3:22-24 . Fundisho la kwamba watenda-dhambi hawawezi kufa katika kuzimu lilitoka kwa Shetani na sio la kweli kabisa. Mungu alizuia jambo hili dhambi ilipoingia katika dunia hii kwa kuulinda mti wa uzima.

**Biblia Wazi - Waovu Wafutiliwa mbali**

Biblia inasema waovu watapatwa na "kifo" ( Waroma 6:23 ), "wataangamizwa" ( Ayubu 21:30 ), "wataangamia" ( Zaburi 37:20 ), 'watateketea' ( Yoh. Malaki 4:1 ), "wataangamizwa pamoja" ( Zaburi 37:38 ), "wataangamizwa" ( Zaburi 37:20 ), "watakatiliwa mbali" ( Zaburi 37:9 ), "watauawa" ( Malaki 4:20 ) Zaburi 62:3 ). Mungu "atawaangamiza" ( Zaburi 145:20 ), na "moto utawala" ( Zaburi 21:9 ). Kumbuka kwamba marejeo haya yote yanaweka wazi kwamba waovu wanakufa na kuangamizwa. Hawaishi milele katika taabu.

Wakati wa mwisho wa dunia, moto utaanguka kutoka mbinguni juu ya waovu na kuwateketeza.

**6. Moto wa mateso utawashwa lini na kwa jinsi gani?**

“Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia hii. Mwana wa Adamu ... atawatupa katika tanuru ya moto.” Mathayo 13:40-42 . “Wakapanda juu ya upana wa nchi, wakaizunguka kambi ya watakatifu, na mji ule uliopendwa; na moto ukashuka kutoka kwa Mungu mbinguni, ukawala.” Ufunuo 20:9 . “Mwenye haki atalipwa duniani; Mithali 11:31 .

**Jibu:** Mwishoni mwa dunia, Mungu Mwenyewe atawasha moto wa Jehanamu. Mji mtakatifu unaposhuka kutoka kwa Mungu kutoka mbinguni ( Ufunuo 21:2 ), waovu hujaribu kuuteka. Wakati huo, Mungu atanyesha moto kutoka mbinguni juu ya dunia, nao utateketeza waovu. Moto huu ni jehanamu ya Biblia.

Kuzimu kutakuwa na moto duniani kote. Itakuwa maili 25,000 kwa mduara wa dunia--joto lake kubwa sana kwamba kila kitu duniani “kitateketezwa”.

**7. Moto wa mateso utakuwa mkubwa kiasi gani na joto kiasi gani?**

“Siku ya Bwana itakuja kama mwivi wakati wa usiku; ambayo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketezwa. .” 2 Petro 3:10 .

**Jibu:** Moto wa Jahannamu utakuwa mkubwa sawa na dunia hii kwa sababu itakuwa ni ardhi inayowaka moto. Moto huu utakuwa wa moto sana kiasi cha kuyeyusha dunia na kuteketeza “kazi zote zilizomo ndani yake.” Mbingu za anga zitalipuka na “kupita kwa kelele kubwa.”

Yesu atasisitiza kutendewa kwa haki kwa waovu. Kiwango chao cha adhabu kitakuwa sawa na kwa mujibu wa matendo yao kama alivyoahidi.

**8. Waovu watateseka motoni hadi lini?**

“Na tazama, Naja upesi, na ujira Wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.” Ufunuo 22:12 . “Ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.” Mathayo 16:27 . “Yule mtumwa aliyejua mapenzi ya bwana wake, na ... wala hakufanya sawasawa na mapenzi yake, atapigwa mapigo mengi. Lakini yeye asiyejua, na kufanya yanayostahili mapigo, atapigwa kidogo.” Luka 12:47 , 48 .

**Jibu:** Biblia haisemi ni muda gani waovu wataadhibiwa kabla ya kupokea kifo motoni. Hata hivyo, Mungu anataja waziwazi kwamba wote wataadhibiwa kulingana na matendo yao. Hii ina maana wengine watapata adhabu kubwa kuliko wengine, kulingana na kazi zao.

Mungu ataumba upya ulimwengu mpya ambao hautaonekana tena na maovu ya zamani ya ulimwengu huu.

**9. Je, moto utazimika hatimaye?**

“Tazama, watakuwa kama makapi; moto utawateketeza; hawatajiokoa na nguvu

za mwali wa moto; Isaya 47:14 . “Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya.” “Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.” Ufunuo 21:1 , 4 .

**Jibu:** Ndiyo, kwa hakika, Biblia inafundisha hasa kwamba moto wa mateso utazimika na kwamba hautasalia “kaa la kuota moto, wala moto wa kukaa mbele yake.” Biblia pia inafundisha kwamba katika ufalme mpya wa Mungu “mambo yote ya kwanza” yatapitilia mbali. Kuzimu, ikiwa ni moja ya vitu vya zamani, imejumuishwa, kwa hivyo tunayo ahadi ya Mungu kwamba itafutwa.

**Je, Mungu ni Mtesaji?**

Ikiwa Mungu angewatesa adui Zake katika chumba cha kutisha milele na milele, Angekuwa mkatili na asiye na huruma kuliko wanadamu ambao wamewahi kuwa katika ukatili mbaya zaidi wa vita. Jehanamu ya milele ya mateso ingekuwa jehanamu kwa Mungu pia, ambaye anampenda hata mwenye dhambi mbaya zaidi.

Moto utawaka hadi majivu tu yatabaki. Hata mifupa itatoweka kabisa.

**10. Ni nini kitakachobaki moto ukizimika?**

“Kwa maana, tazama, siku inakuja, inawaka kama tanuru; na wote wenye kiburi, naam, na wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi; haitawaachia mzizi wala tawi.” “Nanyi mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu katika siku ile niifanyayo, asema Bwana wa majeshi.” Malaki 4:1 , 3 .

**Jibu:** Angalia mstari huo hausemi waovu wataungua kama asbestos ambayo haiungui, kama wengi wanavyoamini leo, bali kama makapi, ambayo yatateketezwa. Neno dogo “juu” linamaanisha kukamilika. Hakuna chochote isipokuwa majivu kitakachosalia wakati moto utazima. Katika Zaburi 37:10 , 20 , Biblia inasema waovu watapanda moshi na kuangamizwa kabisa.

Moto kutoka mbinguni utawashukia waovu na kuwaangamiza, mwili na roho pia.

**11. Je, waovu wataingia kuzimu wakiwa na umbo la mwili na kuangamizwa nafsi na mwili pia?**

“Yakufaa kiungo chako kimoja kipotee wala mwili wako mzima usitupwe katika jehanum.” Mathayo 5:30 . “Afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanum.” Mathayo 10:28 . “Roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa.” Ezekieli 18:20 .

**Jibu:** Ndiyo. Watu halisi, walio hai huingia kuzimu wakiwa na umbo la mwili na kuangamizwa nafsi na mwili pia. Moto kutoka kwa Mungu huko mbinguni utawaangukia watu halisi na kuwaondoa kabisa.

Ibilisi ataangamizwa kabisa kwa moto.

**12. Je, shetani atakuwa msimamizi au bosi wa moto ya mateso?**

“Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika lile ziwa la moto.” Ufunuo 20:10 . “Nitakuleta katika majivu juu ya nchi, machoni pa wote wakutazamao. ...

Wala hutakuwapo tena." Ezekieli 28:18 , 19 .

**Jibu:** Hapana kabisa! Ibilisi atatupwa motoni, nao utamgeuza kuwa majivu.

**13. Je, neno "kuzimu" kama linavyotumiwa katika Biblia hurejelea sikuzote mahali pa kuchomwa moto au adhabu?**

**Jibu:** Hapana, neno "kuzimu" limetumika mara 54 katika Biblia, na katika matukio 12 tu linarejelea "mahali pa kuchomwa moto."

**Neno "kuzimu" limetafsiriwa kutoka kwa maneno kadhaa tofauti na maana tofauti, kama inavyoonyeshwa hapa chini:**

**KATIKA AGANO LA KALE**
mara 31 kutoka "Sheoli," ambalo linamaanisha kaburi."
**KATIKA AGANO JIPYA**
mara 10 kutoka "Hadesi," ambalo linamaanisha "kaburi."
Mara 12 kutoka "Gehena," ambalo linamaanisha "mahali pa kuchomwa moto. "
Mara 1 kutoka "Tartarus," ambayo inamaanisha "mahali pa giza."
54 Jumla yake yote

***Kumbuka:*** *Neno la Kigiriki "Gehena" (iliyotajwa hapo juu) ni tafsiri ya Kiebrania "Ge-Hinnom," ambayo ina maana "Bonde la Hinomu." Bonde hili, ambalo liko kusini na magharibi mwa Yerusalemu, lilikuwa mahali ambapo wanyama waliokufa, takataka, na uchafu mwingine ulitupwa. Moto uliwaka mara kwa mara, kama inavyofanika katika maeneo ya kisasa ya kutupia takataka. Biblia inatumia "Gehena" au "Bonde la Hinomu" kama ishara ya moto utakaoangamiza waliopotea mwisho wa nyakati. Moto wa Gehena haukuisha. Vinginevyo ingekuwa bado inawaka kusini-magharibi mwa Yerusalemu leo. Wala moto wa kuzimu hautaisha.*

Kuangamiza dhambi, wenye dhambi, na Shetani ndiyo njia pekee ya kufanya ulimwengu kuwa salama kwa umilele.

**14. Mungu ana kusudi gani hasa katika moto wa mateso?**

"Ondokeni Kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake. Mathayo 25:41 . "Na iwapo mtu ye yote ambaye hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto." Ufunuo 20:15 . "Kwa maana bado kitambo kidogo tu wasio haki hatakuwepo." "Adui za Bwana ... watateketea; watatoweka na kuwa moshi." Zaburi 37:10 , 20 .

**Jibu:** Kusudi la Mungu ni kwamba jehanamu itamwangamiza shetani na dhambi zote na wenye dhambi na kuifanya dunia kuwa salama milele. Mtenda-dhambi mmoja, ikiwa angeachwa kwenye sayari hii, angekuwa kirusi ambukizi na hatari kinachotishia ulimwengu milele. Ni mpango wa Mungu kuitenga dhambi na kuifuta ili isiwepo milele.

**Kuzimu ya Milele Ingedumisha Dhambi**

Jehanamu ya milele ya mateso ingeendeleza dhambi na kufanya kutokomezwa kwake kusiwezekane. Jehanamu ya milele ya mateso si sehemu ya mpango mkuu

wa Mungu hata kidogo. Nadharia hiyo ya kutisha ni kashfa dhidi ya Jina takatifu la Mungu Mwenye upendo. Ibilisi anafurahi kuona Muumba wetu Mwenye upendo akifafanuliwa kuwa mtawala mkatili sana, na ni yeye pekee anayeweza kufaidika na mafundisho hayo.

**Kuzimu ya Milele Nadharia Iliyoundwa na Mwanadamu**

Nadharia ya "jehanamu ya milele ya mateso" haikutoka katika Biblia, bali imetoka kwa watu wenye mafundisho mapotofu ambao (labda bila kukusudia) waliongozwa na shetani. Na, kwa bahati njema, hakuna mtu atakayekuwa mbinguni kwa sababu anaogopa Jehanamu. Watu wanaokolewa kwa sababu wanampenda na kumtii Kristo.

Yesu atahuzunika sana atakapowaangamiza wale ambao alikufa ili kuwaokoa.

**15. Je, kazi ya kuwaangamiza wenye dhambi si ngeni kwa asili ya Mungu?**

"Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu, bali aghairi mtu mbaya na kuiacha njia yake mbaya, akaishi; ghairini, ziacheni njia zenu mbaya; Ezekieli 33:11 . "Kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa." Luka 9:56 . "Kwa maana Bwana atasimama ... ili afanye kazi yake, kazi yake ya ajabu/ngeni; na kutimiza tendo Lake, tendo Lake la ajabu/geni." Isaya 28:21 .

**Jibu:** Ndiyo, kazi ya Mungu daima imekuwa kuokoa badala ya kuharibu. Kazi ya kuwaangamiza waovu katika moto wa mateso ni ngeni sana kwa asili ya Mungu hivi kwamba Biblia inaiita "tendo Lake la ajabu/geni au Kingereza 'Strange act'." Moyo mkuu wa Mungu utaumia kwa kuangamizwa kwa waovu. Loo, jinsi anavyofanya kazi kwa bidii kila wakati ili kuokoa kila nafsi! Lakini ikiwa mtu ataukataa upendo Wake na kung'ang'ania dhambi, Mungu hatakuwa na chaguo jingine isipokuwa kumwangamiza mtenda-dhambi kwa dhambi yake wakati atakapoondoa ulimwenguni ugonjwa wa kansa ya dhambi unaotisha katika moto wa siku ya mwisho.

Baada ya watenda-dhambi kuharibiwa, Mungu atawaumbia watu Wake dunia mpya yenye kupendeza, ambamo wataishi milele kwa amani, shangwe, na upendo. Dhambi haitainuka tena.

**16. Mikakati ya Mungu baada ya kuzimu kwaajili ya dunia na watu Wake ni ipi?**

"Yeye atakomesha kabisa; taabu haitainuka mara ya pili." Nahumu 1:9 . "Kwa maana, tazama, Mimi naumba mbingu mpya na nchi mpya, na mambo ya kwanza hayatakumbukwa, wala hayataingia moyoni." Isaya 65:17 . "Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, Naye atafanya maskani Yake pamoja nao, nao watakuwa watu Wake, na Mungu Mwenyewe atakuwa pamoja nao, Naye atakuwa Mungu wao, hakutakuwa na mauti tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena." Ufunuo 21:3 , 4 .

**Jibu:** Baada ya moto wa kuzimu kuzimika, Mungu ataumba dunia mpya na

urejeshwaji wa watu Wake pamoja na uzuri na utukufu wote wa Edeni kabla ya dhambi kuingia utafanyika. Mambo ya kutisha ya dhambi yaliyopita yatasahauliwa. Maumivu, kifo, maafa, ole, machozi, magonjwa, tamaa, huzuni na dhambi zote zitafukuzwa milele.

**Dhambi Haitainuka Tena**

Mungu anaahidi kwamba dhambi haitatokea tena. Watu Wake watajawa na amani kamilifu, upendo, shangwe, na kuridhika. Maisha yao ya furaha kamili yatakuwa yenye utukufu na kusisimua zaidi kuliko ambavyo maneno yanayoweza kueleza. Mkasa halisi wa Jehanamu upo katika kukosa mbingu. Mtu ambaye anashindwa kuingia katika ufalme huu mzuri amefanya chaguo la kusikitisha zaidi maishani.

**17. Ninashukuru kujifunza kwamba Mungu hawaadhibu waovu milele katika moto wa mateso.**

**Jibu:**

## MASWALI YA KUFIKIRIA NA KUCHEUA

**1. Je, Biblia haisemi kuhusu "mateso ya milele"?**

Hapana, maneno "mateso ya milele" hayapatikani katika Biblia.

**2. Basi, kwa nini Biblia inasema kwamba waovu wataangamizwa kwa moto usiozimika?**

Moto usiozimika ni moto ambao hauwezi kuzimwa, lakini ambao huzima wakati kila kitu kimegeuka kuwa majivu. Yeremia 17:27 inasema Yerusalemu itaangamizwa kwa moto usiozimika, na katika 2 Mambo ya Nyakati 36:19-21 Biblia inasema moto huu uliunguza mji "ili kutimiza Neno la Bwana kwa kinywa cha Yeremia" na kuuacha ukiwa. Lakini tunajua moto huu ulizimika, kwa sababu Yerusalemu haiwaki leo.

**3. Je, Mathayo 25:46 haisemi waovu watapata "adhabu ya milele"?**

Angalia neno ni *adhabu,* sio *kuadhibu.* Adhabu ingekuwa inaendelea, wakati adhabu ni tendo moja. Adhabu ya waovu ni *kifo,* na kifo hiki ni cha milele.

**4. Je, unaweza kueleza Mathayo 10:28 : "Msiwaogope wauao mwili, wasiweze kuiua roho"?**

Neno "nafsi" lina maana tatu katika Biblia: (1) kiumbe hai— Mwanzo 2:7 , (2) akili— Zaburi 139:14 , na (3) uhai— 1 Samweli 18:1 , ambayo hapa inarejelea uzima wa milele ambao Mungu huwahakikishia wote wanaoufikia ufalme Wake. Hakuna mtu anayeweza kuchukua hii. Sehemu ya mwisho ya Mathayo 10:28 inasema vyote viwili nafsi na mwili vitaangamizwa kuzimu.

**5. Mathayo 25:41 inazungumza juu ya "moto wa milele" kwa waovu. Je,**

**unazimika?**

Ndiyo, kulingana na Biblia, utazimika. Ni lazima tuache Biblia ijieleze yenyewe. Sodoma na Gomora ziliharibiwa kwa moto udumuo milele, au wa milele ( Yuda 7 ), na moto huo ukageuza vyote "kuwa majivu" kuwa onyo/ilani kwa "wale ambao baadaye wangeishi bila kumcha Mungu. 2 Petro 2:6 . Miji hii haiungui leo. Moto ulizima baada ya kila kitu kuteketea. Vivyo hivyo, moto wa milele utazimika baada ya kuwafanya waovu kuwa majivu ( Malaki 4:3 ). Madhara ya moto ni ya milele, lakini kuungua kwenyewe si kwa milele.

**6. Je, hadithi ya tajiri na Lazaro katika Luka 16:19-31 haifundishi jehanamu ya mateso ya milele?**

Hapana, kwa kweli! Ni mfano tu unaotumiwa kusisitiza jambo fulani. Mambo mengi yanaweka wazi kuwa huu ni mfano. Angalia machache kama ifuatavyo:

**A.** Kifua cha Ibrahimu si mbinguni ( Waebrania 11:8-10 , 16 ).

**B.** Watu walio kuzimu hawawezi kuzungumza na walio mbinguni ( Isaya 65:17 ).

**C.** Wafu wako makaburini mwao ( Ayubu 17:13 ; Yohana 5:28 , 29 ). Tajiri alikuwa na umbo la mwili akiwa na macho, ulimi n.k., lakini tunajua kwamba mwili hauendi kuzimu wakati wa kufa. Ni dhahiri sana kwamba mwili unabaki kaburini, kama Biblia inavyosema.

**D.** Wanadamu watapewa thawabu katika ujio wa pili wa Kristo, na sio kifo ( Ufunuo 22:11 , 12 ).

**E.** Waliopotea wanaadhibiwa Jehanamu mwisho wa dunia, na sio wanapokufa ( Mathayo 13:40-42 ). Hoja ya kisa inapatikana katika mstari wa 31 wa Luka 16. Mifano hii haiwezi kuchukuliwa kihalisi (figure of speech). Ikiwa tulichukua mifano halisi, basi lazima pia tuamini kwamba miti huzungumza! (Angalia mfano huu katika Waamuzi 9:8-15 .)

7. **Lakini Biblia husema juu ya waovu kuteswa "milele," sivyo?**

Neno "milele," kama linavyotumiwa katika Biblia, linamaanisha kipindi cha wakati, chenye mipaka au kisicho na mipaka. Neno hili limetumiwa mara 56 katika Biblia kuhusiana na mambo ambayo tayari yamekwisha. (Ili kuangalia katika kamusi ya Biblia yaani Concordance, tafuta neno "ever/milele.") Ni kama neno "tall/mrefu," linalomaanisha kitu tofauti katika kueleza wanadamu, miti, au milima. Katika Yona 2:6 , "forever/milele" wakati wa Yona ndani ya tumbo la samaki inamaanisha "siku tatu mchana na usiku." (Angalia pia Yona 1:17 .) Katika Kumbukumbu la Torati 23:3 , hili linamaanisha "vizazi 10." Kwa upande wa mwanadamu, hii ina maana "muda wote anapoishi" au "mpaka kifo." (Angalia 1 Samweli 1:22 , 28 ; Kutoka 21:6 ; Zaburi 48:14 .) Kwa hiyo waovu waungua moto muda wote wanapokuwa hai, au mpaka kifo. Adhabu hii ya moto ya dhambi itatofautiana kulingana na kiwango cha dhambi cha kila mtu, lakini baada ya adhabu, moto utazimika. Fundisho la

mateso ya milele limefanya mengi zaidi kuwasukuma watu kwenye ukafiri yaani kusema Mungu hayupo na wenda wazimu kuliko ubunifu mwingine wowote wa shetani. Ni kashfa juu ya tabia ya upendo mwororo wa Baba wa mbinguni, Mwenye neema na imefanya madhara makubwa kwa kusudi na kazi ya Kikristo.

## MASWALI YA CHEMSHA BONGO, KWIZZ

**1. Wenye dhambi wanatupwa motoni (1)**
_____ Wanapokufa.
_____ Mwisho wa dunia.
_____ Kwa shetani.

**2. Thawabu ambayo wenye dhambi watapata katika moto wa Jehanamu ni (1)**
_____ Kifo.
_____ Mateso ya milele.
_____ Kuteswa na shetani, ambaye ndiye mtawala.

**3. Moto wa Jehanamu (1)**
_____ Ulimwengu wote utachomwa moto na Mungu.
_____ Unawaka sasa.
_____ Unachoma katika enzi zisizo na mwisho za milele.

**4. Wenye dhambi waliokufa wako (1)**
_____ Toharani/purgatory.
_____ Moto wa Kuzimu.
_____ Makaburi yao.

**5. Idadi ya watu wa kuzimu leo (1)**
_____ Ni sifuri kabisa.
_____ Nambari katika mamilioni.
_____ Haiwezi kubainishwa.

**6. Moto wa Jehanamu (1)**
_____ Unaharibu mwili wa waovu tu.
_____ Hutesa roho za waovu milele.
_____ Huharibu wenye dhambi -nafsi na mwili- na kuwageuza majivu, kisha huzimika.

**7. Jehanamu ya milele ya mateso (1)**
_____ Ni sehemu muhimu sana ya mpango mkuu wa Mungu.
_____ Ni fundisho la shetani na ni kashfa juu ya Jina takatifu la upendo la Mungu, ambaye huchukia kuona watu wakiteseka
_____ Humpa Shetani kibarua milele.

**8. “Kuzimu” katika Biblia (1)**
_____ Daima inarejelea mahali pa kuchomwa moto.
_____ Ina maana kadhaa, mojawapo ikiwa ni *kaburi* .

_____ Inarejelea vyumba vya mateso vya Shetani vilivyo chini ya ardhi.

**9. Kusudi la kuzimu ni (1)**
_____ Kuwalipa na kuwatesa adui za Mungu.
_____ Watu waogopeshe na wawe wema.
_____ Kufuta kabisa dhambi na uovu kutoka kwenye ulimwengu na kuwafanya wenye haki kuwa salama milele.

**10. Kuangamiza watu kuzimu (1)**
_____ Kutakuwa furaha kwa Mungu mkuu wa mbinguni.
_____ Linaitwa 'tendo la ajabu' la Mungu, kwa sababu ni geni sana kwa mpango Wake wa upendo na kuokoa watu.
_____ Itakuwa kazi ya shetani, kwa ushirikiano na mkakati wa Mungu.

**11. Baada ya moto wa kuzimu kuzimika (1)**
_____ Mungu atamfukuza Shetani kwenye anga ya mbali.
_____ Mungu atafanya dunia mpya kamilifu, ambapo dhambi haitatokea tena, na kuwapa watu Wake waishi humo.
_____ Wenye haki wataishi kwa hofu ya kufufuka kwa dhambi tena.

**12. Hadithi ya tajiri na Lazaro (1)**
_____ Ni mfano (allegory) na haupaswi kuchukuliwa kihalisi.
_____ Ni uthibitisho wa Biblia kwa mafundisho ya mateso ya milele.
_____ Inathibitisha kwamba roho zilizo kuzimu zinaweza kuzungumza na za roho zilizo mbinguni.

**13. Neno "milele" kama linavyotumika katika Biblia hurejelea maisha ya mwanadamu (1)**
_____ Ikimaanisha 'wakati usio na mwisho'.
_____ Ni jambo la ajabu na haliwezi kueleweka.
_____ Kwa kawaida humaanisha 'maisha ya mtu', au 'mpaka afe'.

## Miaka 1000 ya Amani

### Somo la 12

Unaweza kuwa na hakika kwamba inakuja - milenia ya ajabu ambayo itaingizwa baada ya kurudi kwa Kristo. Na shetani hataki ujue kuhusu kifungo chake cha miaka 1,000 kwa sababu inadhihirisha tabia yake halisi. Kwa kweli, Shetani ametunga ujumbe wa uongo juu ya milenia ili kukuhadaa! Ni utafiti mzuri na wa kuvutia ambao utatikisa kabisa kila kitu ambacho umewahi kukijua! Sasa unaweza kuwa na Kweli za ajabu za Biblia kuhusu utawala unaokuja wa miaka 1,000.

**1. Ni tukio gani linaloanza kipindi hiki cha miaka 1,000?**
"Hawa wakawa hai tena wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu." Ufunuo 20:4 , NEB, sehemu ya mwisho ya mstari.
**Jibu: Ufufuo huanza kipindi cha miaka 1,000.**

Kipindi cha miaka 1000 huanza wakati wa ufufuo wa wenye haki.

**2. Ufufuo huu unaitwaje? Nani atainuliwa katika huo?**
"Huu ndio ufufuo wa kwanza. Heri na mtakatifu ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza." Ufunuo 20:5 , 6 .
**Jibu:** Unaitwa ufufuo wa kwanza. Watu waadilifu—"heri na watakatifu" wa nyakati zote—watafufuliwa humo.
Kipindi cha miaka 1000 kinaishia kwenye ufufuo wa waovu.

**3. Biblia inasema kuna ufufuo mbili. Ufufuo wa pili ni lini, na ni nani watakaofufuliwa humo?**
"Hao wafu waliosalia [wale waliokuwa waovu] hawakuishi tena hata ile miaka elfu itimie." Ufunuo 20:5 . "Wote waliomo makaburini wataisikia sauti Yake, nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliofanya mabaya kwa ufufuo wa hukumu." Yohana 5:28 , 29 .

**Jibu:** Ufufuo wa pili unafanyika mwishoni mwa kipindi cha miaka 1,000. Waovu watafufuliwa katika ufufuo huu. Unaitwa ufufuo wa laana au aibu.

**Tafadhali angalia:** Ufufuo wa wenye haki huanza miaka 1,000. Ufufuo wa waovu unamaliza miaka 1,000.
Tetemeko la ardhi lenye uharibifu na mvua ya mawe itapiga dunia wakati wa ujio wa pili wa Yesu. Wakati huo wenye haki wa nyakati zote watainuka kukutana na Yesu angani.

**4. Ni matukio gani mengine muhimu yanayotukia miaka 1,000 inapoanza?**
"Tazama, Yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona." Ufunuo 1:7 . "Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, ... na waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza: Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani. " 1 Wathesalonike 4:16 , 17 . "Kukawa na tetemeko kuu la nchi, ambalo tangu wanadamu kuwako juu ya nchi ambalo halijakuwa namna hiyo, na tetemeko kuu namna hii. "Kila kisiwa kikakimbia, wala milima haikuonekana.....
Na mvua ya mawe kubwa ikaanguka kutoka mbinguni juu ya wanadamu, kila jiwe lenye uzani wa talanta moja [makadirio ya wanazuoni yanatofautiana kutoka pauni 58 hadi 100]." Ufunuo 16:18 , 20 , 21 . (Angalia pia Yeremia 4:23-26) ; Isaya 24:1, 3 , 19 , 20 ; Isaya 2:21 .)

**Jibu:** Matukio mengine makubwa yanayotokea miaka 1,000 inapoanza ni: tetemeko la ardhi na mvua ya mawe yenye uharibifu zaidi katika historia itaipiga dunia; Yesu anarudi katika mawingu kwa ajili ya watu Wake; na watakatifu wote nao wananyakuliwa juu angani ili kumlaki Yesu.

Waovu walio hai watauawa kwa mwangaza wa kuja kwa Yesu mara ya pili.

**5. Nini kinatokea kwa waovu--hai na wafu wakati wa kuja kwa Yesu?**
"Kwa pumzi ya midomo Yake atawaua waovu." Isaya 11:4 . "Bwana Yesu

atakapofunuliwa kutoka mbinguni pamoja na malaika Zake wenye nguvu, katika mwali wa moto akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu." 2 Wathesalonike 1:7 , 8 . "Waovu na waangamie mbele za uso wa Mungu." Zaburi 68:2 . "Lakini hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu." Ufunuo 20:5 .

**Jibu:** Waovu walio hai watauawa na uwepo wa Kristo katika ujio wa pili. Malaika alipotokea kwenye kaburi la Yesu, kundi zima la walinzi wa Kirumi lilianguka kama watu waliokufa ( Mathayo 28:2 , 4 ). Mwangaza wa malaika wote, Mungu Baba, na Mungu Mwana watakapoungana, waovu watakufa kana kwamba wamepigwa na umeme. Waovu ambao tayari wamekufa Yesu atakaporudi watabakia makaburini mwao hadi mwisho wa ile miaka 1,000.

Wenye haki watakuwa mbinguni pamoja na Yesu katika muda wa miaka 1,000.

**6. Wengi wanaamini wale ambao hawajaokoka watapata fursa ya kutubu katika muda wa miaka 1,000. Biblia inasema nini kuhusu hili?**

"Waliouawa na Bwana siku hiyo watakuwapo toka upande mmoja wa dunia hata upande wa pili wa dunia; hawataliliwa, wala kukusanywa, wala kuzikwa; watakuwa samadi juu ya nchi." Yeremia 25:33 . "Nilitazama, na tazama, hapakuwa na mtu." Yeremia 4:25 .

**Jibu:** Haiwezekani kwa mtu yeyote kutubu katika muda wa miaka 1,000 kwa sababu hakutakuwa na mtu aliye hai duniani. Wenye haki wote watakuwa mbinguni. Waovu wote watakuwa wamelala wakiwa wafu juu ya dunia. Ufunuo 22:11 , 12 huweka wazi kwamba kesi ya kila mtu imefungwa kabla Yesu hajarudi. Wale wanaongoja kumpokea Kristo hadi miaka 1,000 ianze watakuwa wamengoja bure.

Dunia, katika hali iliyopasuka, iliyotiwa giza, ni litakuwa mo"shimo lisilo na mwisho" ambamo Shetani atalazimika kukaa kwa muda wa miaka 1,000.

**7. Biblia inasema kwamba Shetani atafungwa katika kuzimu wakati wa miaka 1,000. Shimo hili ni nini?**

"Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu. .... Akalishika lile joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga miaka elfu. mtupeni katika shimo lisilo na mwisho ... mpaka ile miaka elfu itimie." Ufunuo 20:1-3.

**Jibu:** Neno la "shimo lisilo na mwisho" katika Kigiriki cha asili ni "abussos," au shimo. Neno hilohilo limetumika katika toleo la Kigiriki la Agano la Kale katika Mwanzo 1:2 kuhusiana na uumbaji wa dunia, lakini hapo linatafsiriwa "kina." "Nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi." Inavutia kujua habari hizi zaidi!

Maneno "chini," "shimo lisilo na mwisho," na "shimo" hapa yanarejelea kitu kile kile—dunia katika hali yake ya giza kabisa, isiyo na mpangilio kabla Mungu hajaipanga au kuiumba. Yeremia, katika kueleza dunia hii wakati wa miaka 1,000, alitumia takriban maneno yaleyale kama haya katika Mwanzo 1:2 : "bila umbo na utupu," "hakuna nuru," "hakuna mtu," 'nyeusi." Yeremia 4:23 , NW. 25 , 28. Kwa hiyo dunia iliyovunjwa na giza isiyo na watu hai itaitwa shimo lisilo na mwisho, au shimo

lenye kina kirefu, wakati wa miaka 1,000 kama ilivyokuwa hapo mwanzo kabla ya Uumbaji kukamilishwa." Isaya 24:22 pia husema juu ya Shetani na malaika wake wakati wa miaka 1,000 kama "waliokusanywa shimoni" na "kufungwa gerezani." Dunia, katika hali iliyopasuka, iliyotiwa giza, ni "shimo lisilo na mwisho" ambamo Shetani atalazimika kukaa katika muda wa miaka 1,000.

**8. Ni mnyororo gani unaomfunga Shetani? Na Kwa nini amefungwa?**
"Malaika ... akiwa na ... mnyororo mkubwa mkononi mwake ... akamshika ... Shetani, akamfunga miaka elfu, ... akamfunga, akatia muhuri juu yake naye hatawadanganya mataifa tena, hata hiyo miaka elfu itimie." Ufunuo 20:1-3 .
**Jibu:** Mlolongo huo ni lugha ya ishara, mazingira ya kifungo. Kiumbe ambacho ni roho hakiwezi kufungwa kwa mnyororo halisi. Shetani "amefungwa" kwa sababu hana watu wa kudanganya. Waovu wote wamekufa na wenye haki wote wako mbinguni. Bwana anamfungia shetani katika dunia hii ili asiweze kuzunguka-zunguka ulimwenguni akitumaini kupata mtu wa kudanganya. Kumlazimisha shetani kukaa duniani peke yake na mapepo yake kwa miaka elfu moja bila mtu wa kudanganya, kwake itakuwa mnyororo mbaya zaidi uliowahi kutengenezwa kwake.

**KAGUA MATUKIO YALIYOTOKEA MWANZONI WA MIAKA 1,000:**
Tetemeko la ardhi lenye uharibifu na mvua ya mawe ( Ufunuo 16:18-21 Ufunuo 6:14-17 ).
Kuja kwa Yesu mara ya pili kwa watakatifu Wake ( Mathayo 24:30 , 31 ).
Wafu wenye haki waliofufuliwa ( 1 Wathesalonike 4:16 , 17 ).
Wenye haki wakipewa kutokufa ( 1 Wakorintho 15:51-55 ).
Miili iliyopewa haki kama Yesu ( 1 Yohana 3:2 Wafilipi 3:21 ).
Wenye haki wote walinyakuliwa juu mawinguni ( 1 Wathesalonike 4:16 , 17 ).
Waovu hai waliouawa kwa pumzi ya kinywa cha Bwana ( Isaya 11:4 ).
Waovu makaburini hubaki wakiwa wamekufa hadi mwisho wa miaka 1,000 ( Ufunuo 20:5 ).
Yesu anawapeleka wenye haki mbinguni ( Yohana 13:33 , 36 14:1-3 ).
Shetani amefungwa ( Ufunuo 20:1-3 ).

**9. Ufunuo 20:4 inasema kutakuwa na hukumu mbinguni wakati wa miaka 1,000. Kwa ajili ya nini? Nani atashiriki?**
"Nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu ... wakaishi, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu." Ufunuo 20:4 . "Hamjui ya kuwa watakatifu watauhukumu ulimwengu?... Hamjui ya kuwa tutawahukumu malaika?" 1 Wakorintho 6:2 , 3 .

**Jibu:** Wenye haki wa nyakati zote (na pengine hata malaika wema) watashiriki katika hukumu wakati wa miaka 1,000. Kesi za wote waliopotea, akiwemo shetani na malaika zake, zitapitiwa upya.
Hukumu hii itaweka wazi maelezo kuhusu waliopotea kwa kila mtu aliyeokoka. Mwishowe, wote wataona kwamba watu wanafungiwa kutoka mbinguni ikiwa tu hawakutaka kuishi kama Yesu au kuwa pamoja Naye.

**KAGUA MATUKIO NA MASHARTI KATIKA MIAKA 1,000:**
Dunia ikiwa katika hali ya kupigwa na mawe makubwa ya mawe na tetemeko la ardhi lenye uharibifu ( Ufunuo 16:18-21 ) 6:14-17 ).
Dunia katika giza kabisa/shimo lisilo na mwisho ( Yeremia 4:23 , 28 ).
Shetani na malaika zake walilazimishwa kukaa duniani/ kufungwa (Ufunuo 20:1-3).
Wenye haki mbinguni wakishiriki katika hukumu ( Ufunuo 20:4 ).
Waovu wote wamekufa ( Yeremia 4:25 Isaya 11:4 ).
Wakati wa miaka 1,000, kila nafsi ambayo imewahi kuishi duniani itakuwa katika mojawapo ya sehemu mbili: (1) duniani, imekufa na kupotea, au (2) mbinguni, ikishiriki katika hukumu. Bwana anakualika uwe mbinguni. Tafadhali ukubali mwaliko Wake.
Jiji takatifu, pamoja na watu wote wa Mungu, litashuka duniani mwishoni mwa ile miaka 1,000.

**10. Mwishoni mwa miaka 1,000 mji mtakatifu, Yerusalemu mpya, utashuka kutoka mbinguni hadi duniani. Nani atakuja nayo? Itatua wapi?**
“Nami Yohana nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu mbinguni.... Nikasikia sauti kuu kutoka mbinguni ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu. Ufunuo 21:2 , 3 . “Tazama, siku ya Bwana inakuja.” “Na miguu Yake itasimama siku hiyo juu ya mlima wa Mizeituni, ulio mbele ya Yerusalemu upande wa mashariki, na mlima wa Mizeituni utapasuka katikati Yake ... Na Bwana, Mungu wangu, atakuja, na watakatifu wote. pamoja Naye.” “Nchi yote itageuzwa kama nchi tambarare kutoka Geba mpaka Rimoni kusini mwa Yerusalemu. Zekaria 14:1 , 4 , 5 , 10 .
**Jibu:** Yerusalemu mpya itakaa mahali ambapo mlima wa Mizeituni umesimama sasa. Mlima huo utasawazishwa na kufanya tambarare kubwa, ambapo mji utakaa juu yake. Watu wote wenye haki wa nyakati zote ( Zekaria 14:5 ), malaika wa mbinguni ( Mathayo 25:31 ), pamoja na Mungu Baba ( Ufunuo 21:2 , 3 ) na Mungu Mwana ( Mathayo 25:31 ) watarudi. duniani pamoja na mji mtakatifu kwa ujio maalum wa tatu wa Yesu. Kuja kwa pili kutakuwa kwa watakatifu Wake wa tatu watakuwa pamoja na watakatifu Wake.

**Ujio wa Yesu mara tatu:**
1. Kuja kwa mara ya kwanza, Bethlehemu katika hori.
2. Kuja mara ya pili, katika mawingu mwanzoni mwa miaka 1,000 kuchukua watu Wake mbinguni.
3. Kuja kwa mara y a tatu ni pamoja na mji mtakatifu na watu wote wenye haki mwishoni mwa miaka 1,000.

**11. Ni nini kitakachowapata waovu waliokufa wakati huu? Je, hilo litamwathirije Shetani?**
“Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu.” “Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake, Naye atatoka kwenda kuwadanganya mataifa.” Ufunuo 20:5 , 7 , 8 .

**Jibu:** Mwishoni mwa miaka 1,000 (Yesu atakapokuja mara ya tatu) waovu watafufuliwa. Shetani, akifunguliwa kutoka katika vifungo vyake, basi atakuwa na

dunia iliyojaa watu (mataifa yote ya ulimwengu) wa kudanganya.
Baada ya mji mtakatifu kushuka, watu waovu wa vizazi vyote—pamoja na Shetani kama kiongozi wao—watajaribu kuuteka mji huo.

**12. Shetani atafanya nini wakati huo?**
"Shetani atatoka kwenda kuwadanganya mataifa ... wa dunia, ... kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari. Wakapanda juu ya upana wa bahari. nchi, na kuizingira kambi ya watakatifu, na mji ule uliopendwa." Ufunuo 20:7-9.

**Jibu:** Shetani, sawa na asili yake, mara moja ataanza kusema uongo kwa watu waliobaki duniani - waovu kutoka nyakati zote. Pengine atadai kwamba jiji hilo kweli ni lake, kwamba aliondolewa isivyo haki kutoka katika ufalme wa mbinguni, kwamba Mungu ana tamaa/uchu wa mamlaka na ni mkatili, na kwamba Mungu anajitayarisha kuwaangamiza wote kutoka kwenye uso wa dunia kwa uharibifu wa moto usioepukika. Atawasadikisha kwamba, wakiungana, Mungu hawezi kushinda. Wakiwa wengi yaani kama ulimwengu mzima dhidi ya jiji moja, ushindi utaonekana kuwa ni wa hakika kwao. Kisha mataifa yataungana na kuyapanga majeshi yao kuzunguka Yerusalemu mpya.
Wakati waovu wa nyakati zote wakizingira jiji takatifu, Mungu atawaangamiza kwa moto unaoanguka kutoka mbinguni.

**13. Ni nini kitakachokatiza mkakati wa Shetani wa kuteka au kuharibu jiji hilo?**
"Moto ulishuka kutoka kwa Mungu kutoka mbinguni, ukawala. Ufunuo 20:9 , 10 ; 21:8 . "Waovu ... watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu katika siku ile nitakapofanya haya, asema Bwana wa majeshi." Malaki 4:3 .
**Jibu:** Moto utashuka ghafla kutoka mbinguni (sio kutoka kuzimu, kama wengi wanavyoamini) juu ya waovu na wote watageuka kuwa majivu, ikiwa ni pamoja na shetani na malaika zake (Mathayo 25:41 ) . Moto huu unaoangamiza dhambi na wenye dhambi unaitwa kifo cha pili. Hakuna ufufuo kutoka kwa kifo hiki. Ni hatua ya mwisho. Angalia kuhusu shetani, yeye hatakuwa msimamizi wa moto, kama inavyoaminika. Atakuwa ndani ya moto, na hilo litamfanya asiwepo tena.

**14. Waovu wanapoteketezwa na moto kuzimika, ni tukio gani tukufu na lenye kusisimua litakalofuata?**
"Tazama, Mimi naumba mbingu mpya na nchi mpya." Isaya 65:17 . "Tazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake." 2 Petro 3:13 . "Yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, Tazama, nayafanya yote kuwa mapya." Ufunuo 21:5 . "Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, Naye atafanya maskani Yake pamoja nao, nao watakuwa watu Wake, na Mungu Mwenyewe atakuwa pamoja nao, na kuwa Mungu wao." Ufunuo 21:3 .

**Jibu:** Mungu ataumba mbingu mpya na dunia mpya, na Yerusalemu mpya itakuwa mji mkuu wa dunia nchi mpya. Dhambi na ubaya wake vitatoweka milele. Watu wa Mungu hatimaye watapokea ufalme walioahidiwa. "Watapata furaha na shangwe, huzuni na kuugua vitakimbia." Isaya 35:10 . Ni ajabu isiyo na lugha ya kuelezea!

Itakuwa kitu kibaya kukosa mema haya! Mambo haya yapo karibu sana na kwetu na hivyo hatupaswi kutokuwa na uhakika! Mungu ana mahali palipoandaliwa kwa ajili yako ( Yohana 14:1-3 ). Panga kuishi ndani yake. Yesu anasubiri idhini/kibali chako.

**KAGUA MATUKIO ya MWISHO WA MIAKA 1,000:**
Ujio wa tatu wa Yesu pamoja na watakatifu Wake ( Zekaria 14:5 ).
Mji mtakatifu unakaa juu ya mlima wa Mizeituni, ambao unakuwa tambarare kubwa ( Zekaria 14:4 , 10 ).
Baba, malaika, na wote wenye haki huja pamoja na Yesu ( Ufunuo 21:1-3). Mathayo 25:31 Zekaria 14:5 ).
Wafu waovu wanafufuliwa na Shetani anafunguliwa ( Ufunuo 20:5 , 7 ).
Shetani anaudanganya ulimwengu wote ( Ufunuo 20:8 ).
Waovu wanauzingira mji mtakatifu ( Ufunuo 20:9 ).
Waovu wanaangamizwa kwa moto ( Ufunuo 20:9 ).
Mbingu mpya na nchi ziliumbwa ( Isaya 65:17 2 Petro 3:13 Ufunuo 21:1 ).
Watu wa Mungu wanafurahia umilele pamoja na Kristo katika dunia mpya ( Ufunuo 21:2-4 ).

**MIAKA 1,000 YA UFUNUO 20**
**MATUKIO KATIKA MIAKA 1,000**

1. Dunia iliyopasuka, ukiwa, na giza.
2. Waovu wote wamekufa duniani.
3. Shetani amefungwa hapa duniani.
4. Wenye haki wanahukumu mbinguni.

| UFUFUO WA KWANZA MWANZO WA MIAKA 1,000 | UFUFUO WA PILI KATIKA KARIBU YA MIAKA 1,000 |
|---|---|
| 1. Tetemeko la ardhi lenye uharibifu na mvua ya mawe. | 1. Kuja kwa Yesu mara ya tatu pamoja na watakatifu. |
| 2. Kuja kwa Yesu mara ya pili kwa ajili ya watakatifu. | 2. Mji mtakatifu unashuka kwenye mlima wa Mizeituni, ambao unakuwa tambarare kubwa. |
| 3. Wafu wenye haki wanafufuliwa kwa uzima. | 3. Baba, malaika, na wenye haki wanakuja pamoja na Yesu. |
| 4. Wenye haki wakipewa kutokufa. | 4. Wafu waovu wanafufuliwa na Shetani kufunguliwa. |
| 5. Wenye haki wanapewa miili kama ile ya Yesu. | 5. Shetani huwadanganya mataifa yote. Wanauzunguka mji mtakatifu. |
| 6. Wenye haki wote wananyakuliwa juu mawinguni. | 6. Waovu kuangamizwa kwa moto. |
| 7. Waovu wanaoishi wanakufa kwa uwepo wa Bwana. | 7. Mbingu mpya na nchi zinaumbwa. |
| 8. Waovu tayari katika makaburi yao wakiwa wamekufa. | 8. Watu wa Mungu wanafurahia umilele pamoja na Yesu. |
| 9. Yesu anawachukua wenye haki mbinguni. | |
| 10. Shetani amefungwa. | |

**15. Je, tunaweza kujua ni muda gani Yesu atarudi kwa ajili ya watakatifu Wake?**
"Nanyi myaonapo hayo yote, jueni ya kuwa Yu karibu, milangoni." Mathayo 24:33 . "Mambo hayo yaanzapo kutokea, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa maana ukombozi wenu umekaribia." Luka 21:28 . "Maana ataimaliza kazi, na kuikata kwa haki; Warumi 9:28 . "Kwa maana watakaposema, Kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula. 1 Wathesalonike 5:3.

**Jibu:** Yesu alisema wakati ishara za kuja Kwake zinatimizwa kwa haraka, kama zilivyo leo, tunapaswa kushangilia na kujua kwamba kuja Kwake kumekaribia—hata milangoni. Na mtume Paulo alisema tunaweza kujua mwisho umekaribia wakati kuna harakati kubwa ya amani duniani. Hatimaye, Biblia inasema Mungu ataifupisha kazi hiyo (Warumi 9:28 ). Kwa hivyo bila shaka, tunaishi katika wakati uliokopeshwa. Bwana atakuja kwa ghafula na bila kutazamiwa--katika saa isiyojulikana na mtu yeyote, ila kwa Mungu pekee ( Mathayo 24:36 ; Matendo 1:7 ). Usalama wetu pekee ni kuwa tayari wakati wote.

**16. Hakika ninapanga kuishi katika nyumba ya kupendeza ni ajabu iliyojengwa kwaajili haiba yangu, ambayo Yesu ananiandalia mbinguni.**

**Jibu:**

## MASWALI YA KUFIKIRI NA KUCHEUA

**1. Kipindi kitakuwa cha muda gani tangu siku jiji takatifu litakaposhuka hadi waovu waangamizwe kwa moto kutoka mbinguni?**
Biblia inasema itakuwa majira ya "madogo," au mafupi ( Ufunuo 20:3 ). Wakati wa kutosha utahitajika kwa Shetani kuwashawishi watu kufuata mpango wake na kuandaa silaha za vita. Urefu kamili wa wakati haujafunuliwa katika Maandiko.

**2. Watu watakuwa na miili ya aina gani katika ufalme mpya wa Mungu?**
Biblia inasema waliokombolewa watakuwa na miili kama ile ya Yesu ( Wafilipi 3:21 ). Yesu alikuwa na mwili halisi wa nyama na mifupa baada ya kufufuka Kwake ( Luka 24:36-43 ). Waliookoka hawatakuwa mizimu. Watakuwa watu halisi, wanaoshikika, na kutambulika kama vile Adamu na Hawa walivyokuwa.

**3.Je,BibliainasemajinsiwaliopoteawatakavyotendakatikaujiowapiliwaYesu?**
Ndiyo. Biblia inasema watailia milima na miamba, Tuangukieni, mkatufiche mbali na uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na ghadhabu ya Mwana-Kondoo; kwa maana siku iliyo kuu ya ghadhabu yake imekuja; ni nani atakayeweza kusimama?" Ufunuo 6:16 , 17 . (Ona pia mistari ya 14 na 15.) Kwa upande mwingine, wenye haki watasema, "Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, tuliyemngoja, naye atatuokoa; huyu ndiye Bwana, tumemngoja. , tutashangilia na kuushangilia wokovu wake." Isaya 25:9 .

**4. Mji mtakatifu unaposhuka, je, waovu wataweza kuwaona watu waadilifu walio ndani ya jiji hilo?**
Uwezekano wa kuwaona ni mkubwa. Biblia inasema jiji hilo litaonekana wazi kama bilauri (transparent ) (Ufunuo 21:11 , 18 ). Wenye haki wataweza kuwaona waovu ( Zaburi 37:34 ), na waovu wataweza kuwaona wenye haki ( Luka 13:28 ). Hii inaweza kumaanisha kwamba matukio fulani ya kusikitisha sana yatafanyika kwenye ukuta wa jiji, sehemu iliyookolewa ya familia ikiwa ndani na sehemu iliyopotea nje. Maumivu ya moyo na kiwewe yatakayokuwepo, yote haya ni yanautatiza moyo na hivyo lugha ya binadamu haiwezi kuelezea.

**5. Biblia inasema Mungu atafuta machozi yote katika macho ya watu Wake na hakutakuwa na kifo, huzuni, wala maumivu tena. Haya yatatokea lini?**
Kutoka Ufunuo 21:1-4 na Isaya 65:17 , inaonekana kwamba haya yatatokea baada ya dhambi na wenye dhambi kuharibiwa. Wakati wa hukumu ya mwisho na uharibifu kwa moto, watu wa Mungu watakuwa na sababu nyingi za kupata huzuni nyingi.
Wanapotambua kwamba watu wa ukoo na marafiki zao wamepotea na kwamba watu waliowapenda wanaangamizwa kwa moto, bila shaka uchungu utaleta machozi na huzuni kubwa kwa watu wa Mungu. Lakini baada ya moto kuzimika, Bwana atayafuta machozi yao. Kisha ataumba mbingu mpya na dunia mpya kwa ajili ya watu Wake, ambayo itawaletea shangwe na burudiko na kuridhika kusikoweza kuelezeka. Na huzuni, sikitiko, kilio, na huzuni vitatoweka milele.

**6. Kuharibiwa kwa malaika waovu na watu kutakuwa na matokeo gani juu ya Mungu Baba na Mwana Wake?**

Bila shaka watafarijiwa na kufurahi sana kwamba kansa mbaya ya dhambi imetoweka milele na kwamba ulimwengu uko salama. Hakika wao pia watapata huzuni kubwa, yenye kuukatakata moyo kwa ule uhalisia kwamba wengi wa wale waliowapenda, na ambao Yesu alikufa kwa ajili yao, walichagua kushikamana na dhambi na kukataa wokovu. Shetani mwenyewe wakati mmoja alikuwa rafiki yao binafsi, aliyekuwa mchangamfu kwao na watu wengi katika moto walikuwa watoto wao wapendwa sana. Itakuwa kama ule uchungu wa kushuhudia mmoja wa watoto wako waliokosea akiuawa. Dhambi imekuwa mzigo mzito juu ya Baba na Mwana tangu kuanzishwa Kwake na shetani. Kusudi la Baba na Mwana limekuwa kuwapenda watu na kuwavuta kwa upole kwenye wokovu. Hisia zao zinaonyeshwa katika Hosea 11:8, : "Nitakuachaje, Ee Efraimu?

**7. Yesu ana mwili wa aina gani?**

Ana mwili wa nyama na mifupa. Baada ya kufufuka Kwake, Yesu aliwatokea wanafunzi Wake ( Luka 24:36-43 ) na alionyesha kwamba Yeye hakuwa roho au mzimu kwa kusema kwamba Yeye alikuwa nyama na mifupa, kuwafanya wauguse na kuuhisi mwili Wake, na kwa kula samaki na asali.

**Yesu Anapaa**

Kisha akatembea nao hadi Bethania na, alipokuwa akizungumza nao, alipanda mbinguni ( Luka 24:49-51 ). Malaika aliyewatokea wanafunzi Yesu alipopaa alieleza kwamba "Yesu huyu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda Zake mbinguni." Matendo 1:11 .

**Yesu Huyu Atarudi**

Msisitizo wa malaika ulikuwa kwamba Yesu Huyu Huyu (wa nyama na mifupa) atakuja tena. Atakuwa halisi, sio roho, na watakatifu waliofufuka na kubadilishwa watakuwa na miili kama Wake ( Wafilipi 3:21) . 1 Yohana 3:2 ). Miili ya mbinguni ya watakatifu pia itakuwa isiyoharibika na isiyoweza kufa (1 Wakorintho 15:51-55).

## MASWALI YA CHEMSHA BONGO/KWIZZ

**1. Weka alama kwenye matukio yatakayotokea mwanzoni mwa miaka 1,000 ya Ufunuo sura ya 20: (10)**

_____ Kuja kwa Yesu mara ya pili.
_____ Tetemeko la ardhi na mvua ya mawe.
_____ Wafu waadilifu wanafufuliwa.
_____ Shetani amefungwa.
_____ Waovu hai wauawa.
_____ Mwenye haki akipewa kutokufa.
_____ Mji mtakatifu unashuka.
_____ Wenye haki wanapelekwa mbinguni.
_____ Waovu makaburini wanabaki wamekufa.
_____ Wenye haki wanapewa miili kama ya Yesu.
_____ Wenye haki wananyakuliwa juu mawinguni.

_____ Yesu anaingia Yerusalemu mpya kwa ushindi.

**2. Kila mtu aliye hai duniani atamwona Yesu katika ujio Wake wa mara ya pili. (1)**
_____ Kweli.
_____ Uongo.

**3. Wenye haki watakuwa roho mbinguni. (1)**
_____ Kweli.
_____ Uongo.

**4. Ni kipi kati ya mambo yafuatayo ambacho ni kweli kuhusu kipindi cha miaka 1,000? (2)**
_____ Wenye dhambi wengi wataongoka.
_____ Shetani na malaika zake watalazimika kukaa duniani.
_____ Shetani atafungwa na ukweli kwamba hakuna televisheni ya kutazama.
_____ Kutakuwa na mwanga mkali na jua duniani kwa muda wa miaka 1,000.
_____ Shetani atawafufua waovu waliokufa ili wamsaidie kukaa pamoja naye kwa mazungumzo.
_____ Wenye haki watakuwa mbinguni, wakishiriki katika hukumu.

**5. Ni yapi kati ya yafuatayo yaliyo kweli kuhusu matukio ya mwisho wa kipindi cha miaka 1,000? (4)**
_____ Kristo atakuja kwa mara ya tano.
_____ Mji mtakatifu utatua katika eneo la Cairo.
_____ Malaika na Mungu Baba watakuja pamoja na Yesu.
_____ Waovu watafufuliwa.
_____ Yesu atakuja na watakatifu Wake.
_____ Mungu ataamua kutowainua waovu hata hivyo.
_____ Waovu wataangamizwa na malaika waovu wenye hasira.
_____ Mungu ataumba mbingu mpya na nchi mpya.
_____ Mungu atamfukuza Shetani hadi sehemu za nje za sayari zingine.
_____ Ibilisi ataufuta mji mtakatifu kwa kombora jipya lenye nguvu.

**6. Mnyororo unaomfunga Shetani utakuwa (3)**
_____ Ni mfano wa--mnyonyoro wa mazingira.
_____ Utamlazimisha abaki duniani.
_____ utatengenezwa upya kwa chuma kigumu sana.
_____ Utavunjwa na shetani ndani ya masaa 24.
_____ Utamzuia asiwajaribu watu wa Mungu, ambao watakuwa salama mbinguni.

**7. Ni kauli zipi ambazo ni za kweli kuhusu shimo lisilo na mwisho? (2)**
_____ Ni shimo kubwa ndani ya ardhi.
_____ Inamaanisha shimo lisilo na mwisho.
_____ Inarejelea dunia--yenye giza na isiyo na umbo na yenye utupu.
_____ Ni jina lingine la kuzimu.

**8. Ni mambo gani ambayo ni ya kweli kuhusu ujio wa kwanza, wa pili, na wa tatu wa Yesu? (3)**

_____ Ujio wa kwa kwanza ulikuwa Bethlehemu kama mtoto mchanga.
__ _____Ujio wa Pili ulikuwa katika siku za Nuhu.
_____ Ujio wa pili ulikuwa katika siku za Martin Luther.
_____ Ujio wa pili utakuwa mwanzoni mwa miaka 1,000.
_____ Ujio wa tatu utakuwa mwishoni mwa miaka 1,000.
_____ Ujio wa tatu utakuwa baada ya dunia mpya kuumbwa.

**9. Kifo cha waovu katika ziwa la moto ni kifo cha pili. (1)**
_____ Kweli.
_____ Uongo.

**Mpango wa Afya wa Mungu USIO na Gharama**

**Somo la 13**

Huduma za tiba zina gharama kubwa, isiyoelezeka na wakati mwingine isiyo na kifani - Je, isingekuwa vizuri ikiwa tusingehitaji madaktari tena? Je! unajua kuwa kuna njia iliyothibitishwa ya kuwakosesha madaktari wengi kazi? Tunza mwili wako vizuri! Wanasayansi wametoa maonyo ya hakika kuhusu kolesteroli, tumbaku, msongo, kunenepa kupita kiasi, na pombe, kwa nini wewe ucheze patapotea na baraka zako? Hospitali na taasisi za magonjwa ya akili zimejaa watu ambao wamepuuza maonyo - je, kweli unataka kujiunga nao kwenye mawodi ya hospitali? Mungu anajali sana jinsi unavyoutendea mwili wako, na amekupa mpango wa afya bila gharama, na mwongozo wa kufuata... nao ni Biblia! Kuna Ukweli wa kushangaza kuhusu jinsi unavyoweza kuwa na afya tele na maisha marefu, angalia Mwongozo huu wa Utafiti katika somo hili - lakini hakikisha umeusoma wote bila ya kurukaruka, hadi hitimisho!

**1. Je, kanuni za afya ni sehemu ya dini ya Kweli ya Biblia?**

"Mpenzi natamani ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo." 3 Yohana 2 .

**Jibu:** Ndiyo. Kwa kweli, Biblia huiweka afya katika sehemu ya juu kabisa ya orodha ya mambo yaliyokuwa muhimu. Akili ya mwanadamu, roho yake, na mwili vyote vinahusiana na vinategemeana. Kinachoathiri kimoja ya hivyo huathiri kingine. Ikiwa miili yetu itatumiwa vibaya, akili zetu na maisha yetu ya kiroho haviwezi kuwa kile ambacho Mungu aliamuru kiwe.

**2. Kwa nini Mungu alitoa sheria za afya kwa watu Wake?**

"Bwana akatuamuru kuzifanya amri hizi zote ... kwa faida yetu siku zote, ili atuhifadhi hai." Kumbukumbu la Torati 6:24 . "Nanyi mtamtumikia Bwana, Mungu wenu,

Naye atakibarikia chakula chako, na maji yako; Nami nitakuondolea ugonjwa kati yako." Kutoka 23:25 .

**Jibu:** Mungu alitoa sheria za afya kwa sababu anajua ni nini bora kwa mwili wa mwanadamu. Watengenezaji wa magari huweka "mwongozo wa uendeshaji au manual for operation" katika sehemu ya kidroo cha kila gari jipya kwa sababu wanajua kinachofaa zaidi kwa bidhaa yao waliyoitengeneza na hii pia tunaona tukinunua simu au kitu kingine, tunapata maelezo ya jinsi ya kukitumia kifaa hicho. Mungu, ambaye aliumba miili yetu, pia ana "mwongozo wa uendeshaji wa miili yetu." Inaitwa Biblia Takatifu. Kupuuza "mwongozo wa utendaji" wa Mungu hutokeza magonjwa, mawazo yaliyopotoka, na maisha ya kuteketea, sawa na vile kutumia vibaya gari (kinyume na shauri la mtengenezaji) inavyoleta matatizo makubwa ya gari. Kufuata sheria za Mungu kunaleta "kuokoa afya" ( Zaburi 67:2) na maisha tele zaidi ( Yohana 10:10 ). Sheria hizi kuu za afya ni kama ukuta au uzio wa kuzuia magonjwa ya Shetani. Mungu anatuambia kanuni hizi ni zipi ili tuepuke mitego ya shetani.

Sheria za afya za Mungu zina mengi ya kusema kuhusu kile tunachokula na kunywa.

### 3. Je, sheria za Mungu za afya zinahusiana kwa vyovyote na kula na kunywa?

"Kuleni kilicho kizuri." Isaya 55:2 . "Basi mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu." 1 Wakorintho 10:31 .

**Jibu:** Ndiyo, Mkristo hatakula na kunywa kwa njia tofauti, yote atafanya kwa utukufu wa Mungu, akitumia tu "kile kilicho kizuri." Ikiwa Mungu anasema kitu hakifai kuliwa, lazima awe na sababu nzuri. Yeye si dikteta mkali, lakini ni Baba Mwenye upendo. Mashauri Yake yote ni kwa manufaa yetu daima. Biblia inaahidi hivi: "Hakuna jambo jema ambalo hatawanyima wale wanaotembea kwa unyoofu. Zaburi 84:11 . Basi ikiwa Mungu anatuzuilia kitu, ni kwa sababu si kizuri. Mfano mzuri ni zile amri kumi za Mungu, zote ni kwa faida yetu na zinahusu afya yetu katika nyanja zote. Mfano Mungu anaposema usizini au usifanye uasherati, anasema kwa faida yetu, Yeye hana mke kwamba utamchukulia mke wake, la! Ila jambo hili litaleta huzuni kwenye familia, litaleta magonjwa ya zinaa, na pengine hata kifo kwaajili ya hasira! Nafikiri utakuwa umeanza kuelewa sasa, na amri zote ukienda nazo taratibu kwa kuzichunguza, utaona ni kwaajili ya afya yetu wanadamu. Maana mtu hawezi kuwa na afya kama anagombana na wengine, au anawaonea wengine wivu, au hawaheshimu wazazi wake, au hachukui muda kupumzika Siku ya Saba kama ambavyo Mungu ameagiza.

***Kumbuka:*** *Hakuna mtu anayeweza kula njia yake kwenda mbinguni, yaani chakula bora chenyewe tu hakiwezi kukufanya ukafika mbinguni. Kula hata chakula cha malaika hakutawapa watu haki ya kuingia mbinguni. Ni kumkubali tu Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi ndiyo kunaweza kufanya hivyo. Hata hivyo, kupuuza sheria za afya za Mungu kunaweza kumfanya mtu apotee, kwa sababu kutaharibu hukumu maamuzi yake na kumfanya atende dhambi. Nafikiri unajua kwamba kuweka vitu vingine mdomoni kunabadilisha akili na maamuzi yako.*

Mungu aliagiza chakula cha mboga kwa Adamu na Hawa.

**4. Mungu aliwapa watu kula nini alipowaumba na kuwaandalia mlo kamili?**

"Mungu akasema, Tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu ... na kila mti ... uzaao mbegu." "Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula." Mwanzo 1:29 ; 2:16 .

**Jibu:** Chakula ambacho Mungu aliwapa watu hapo mwanzo kilikuwa ni matunda, nafaka, na jamii ya karanga. Mboga ziliongezwa baadaye kidogo, mwanadamu alipoanguka kama dawa ( Mwanzo 3:18 ).

**5. Ni vitu gani vinavyotajwa hasa na Mungu kuwa najisi na haramu?**

**Jibu:** Katika Mambo ya Walawi 11 na Kumbukumbu la Torati 14, Mungu kwa uwazi kabisa anaonyesha makundi yafuatayo kuwa najisi. Soma sura zote mbili kwa ukamilifu.

**A. Wanyama wote ambao hawana kwato zilizopasuka na kucheua** ( Kumbukumbu la Torati 14:6 )

**B. Samaki wote na viumbe wa majini ambavyo havina mapezi na magamba.** Karibu samaki wote ni safi ( Kumbukumbu la Torati 14:9 ).

**C. Ndege wote wawindao, walao mizoga, na walao samaki** ( Mambo ya Walawi 11:13-20 ).

**D. Wengi "watambaao" (au wanyama wasio na uti wa mgongo) pia ni najisi** ( Mambo ya Walawi 11:21-47 ).

***Kumbuka:*** *Sura hizi zinaweka wazi kwamba wanyama wengi, ndege, na viumbe vya majini ambavyo watu kwa kawaida hula ni safi. Kuna hata hivyo, baadhi ya vitu vichache vinavyojulikana kuwa vinaiwa na watu na si safi . Kulingana na sheria za Mungu, wanyama wafuatao ni najisi na hawapaswi kuliwa: nguruwe, punda, kunguru, mwewe, bata, tembo, kuchakulo, sungura, kambare, kamba, kaa, kamba, pweza, konokono wenye kijumba na wasio na kijumba, nyoka, mbwa, panya, vyura, na wengine wengi.*

**6. Lakini mimi napenda nyama ya nguruwe. Je, Mungu ataniangamiza nikila?**

"Kwa maana, tazama, Bwana atakuja na moto ... na kwa upanga wake Bwana atateta na wote wenye mwili; na waliouawa na Bwana watakuwa wengi. Nao wanaojitakasa na kujitakasa ... wakila nyama ya nguruwe, na machukizo, na panya; watakoma pamoja, asema Bwana.. Isaya 66:15-17 .

**Jibu:** Hili linaweza kushtua, lakini ni kweli na ni lazima tuambiwe. Biblia husema kwa uhakika kwamba wote wanaokula "nyama ya nguruwe," "panya," na vitu vingine vichafu ambavyo ni "chukizo" wataangamizwa kwa moto wakati wa kuja kwa Bwana. Mungu anaposema tuache kitu wala tusikiguse au tusile, tunapaswa kwa njia zote kumtii. Kwani, kula tu kipande cha tunda lililokatazwa kwa Adamu na Hawa, wanandoa hawa wawili wasio na dhambi, walileta dhambi na kifo

kwa ulimwengu huu. Je, kuna mtu yeyote anayeweza kusema haijalishi wakati Mungu anaonyesha waziwazi kwamba kuna maana? Mungu anasema wanadamu wataangamizwa kwa sababu "walichagua nisichopendezwa nacho." Isaya 66:4 .

Dhabihu ya Nuhu ya wanyama safi ( Mwanzo 8:20 ) inaonyesha kwamba alielewa tofauti kati ya safi na najisi.

**7. Lakini je, sheria hii ya wanyama safi na najisi haikuanzia pale Sinai? Je, haikuwa kwa Wayahudi pekee, na haikuishia msalabani?**

"Bwana akamwambia Nuhu, ... Katika kila mnyama aliye safi ujitwalie saba... na katika wanyama wasio safi wawili wawili." Mwanzo 7:1 , 2 .

**Jibu:** Hapana! Biblia ina uthibitisho wa kutosha kwamba kulikuwa na wanyama safi na najisi tangu mwanzo wa Uumbaji. Nuhu aliishi muda mrefu kabla ya Wayahudi wowote kuwepo, lakini alijua juu ya walio safi na wasio safi, kwa sababu aliwaingiza ndani ya safina wanyama walio safi "saba" na wale wasio safi "wawili". Ufunuo 18:2 inawataja baadhi ya ndege kuwa najisi kabla tu ya ujio wa pili wa Kristo.

Kifo cha Kristo hakikuwa na mabadiliko yoyote katika sheria hizi za afya, kwa kuwa Biblia inasema kwamba wote wanaozivunja wataangamizwa wakati Yesu atakaporudi ( Isaya 66:15-17 ). Tumbo la Myahudi na mfumo wa usagaji chakula wake hautofautiani kwa njia yoyote na ule wa Mmataifa. Sheria hizi za afya ni za watu wote kwa wakati wote.

Utumiaji wa vileo unashutumiwa waziwazi na Maandiko.

**8. Je, Biblia inakataza matumizi ya vileo?**

"Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; na adanganyikaye kwa vitu hivyo hana hekima." Mithali 20:1 . "Usiiangalie mvinyo, ikiwa ni nyekundu, inapotoa rangi yake kikombeni, inaposonga vizuri. Hatimaye huuma kama nyoka, na kuchoma kama fira." Methali 23:31 , 32 . "Wala wazinzi ... wala walevi ... hawataurithi ufalme wa Mungu." 1 Wakorintho 6:9 , 10 .

**Jibu:** Ndiyo, Biblia inakataza waziwazi matumizi ya vileo.

**9. Je, Biblia inakataza matumizi ya tumbaku?**

**Jibu:** Ndiyo, Biblia inatoa sababu sita zinazofanya kutumia tumbaku kusimpendeze Mungu:

**A. Utumiaji wa tumbaku unadhuru afya na unachafua mwili.**

"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu huyo kwa kuwa hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi." 1 Wakorintho 3:16 , 17 .

**B. Nikotini ni kitu cha kulevya ambacho huwafanya watu kuwa watumwa.**

Warumi 6:16 inasema kwamba tunakuwa watumwa kwa yeyote (au chochote)

tunachojitolea wenyewe kwa hicho. Watumiaji wa tumbaku ni watumishi au waraibu wa nikotini. Yesu anasema, "Utamwabudu Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye peke yake." Mathayo 4:10 .

**C. Tabia ya tumbaku ni najisi.**

"Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, wala msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha." 2 Wakorintho 6:17 . Ni jambo la upuuzi sana kufikiria Kristo akitumia tumbaku au sivyo? Je, Yesu angefanya nini, angevuta tumbaku unafikiri?

**D. Matumizi ya tumbaku yanapoteza pesa.**

"Mbona mnatoa pesa kwa kitu ambacho si mkate?" Isaya 55:2 . Sisi ni mawakili wa Mungu wa fedha tulizopewa, na "inahitajika katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu." 1 Wakorintho 4:2 .

**E. Utumiaji wa tumbaku kamwe haumsogezi mtu yeyote karibu na Kristo.**
"Jiepusheni na tamaa za mwili zipiganazo na roho." 1 Petro 2:11 . Utumiaji wa tumbaku ni tamaa ya mwili.

**F. Matumizi ya tumbaku yanafupisha maisha.**

Matokeo ya hivi majuzi ya kisayansi yanathibitisha kwa uhakika kwamba matumizi ya tumbaku mara nyingi hupunguza muda wa maisha kwa kiasi cha thuluthi moja. Hii inavunja amri ya Mungu dhidi ya kuua ( Kutoka 20:13 ). Ingawa ni mauaji ni ya polepole, bado ni mauaji. Mojawapo ya njia bora za kuahirisha mazishi yako ni kuacha kutumia tumbaku. Na wale wanaokuzunguka pia unawaathiri kwa moshi wa tumbaku unapovuta zaidi yako mwenyewe, Je, tumeona hata serikali nyingi zimepiga marufuku kuvuta tumbaku kwenye majengo yake, je wewe uliye muumini inakuwaje unaendelea bado kuvuta tumbaku?

**10. Ni zipi baadhi ya sheria sahili ila ni muhimu sana, za afya zinazopatikana katika Biblia?**

**Jibu: Hapa kuna sheria 11 za afya za Biblia:**

**A. Kula milo yako kwa nyakati maalumu, usile katikakati ya miilo, pishanisha muda, usile siku nzima kama ng'ombe anayecheua chakula na usitumie mafuta ya wanyama au damu.**
"Kula kwa wakati wake." Mhubiri 10:17. "Itakuwa ni amri ya milele ... kwamba msile mafuta wala damu." Mambo ya Walawi 3:17 .

***Kumbuka:*** *Uchunguzi wa hivi karibuni wa kisayansi umethibitisha ukweli kwamba mashambulizi mengi ya moyo yanatokana na kiwango cha juu cha cholesterol katika damu, na kwamba matumizi ya "mafuta" yanahusika sana na kiwango hiki cha juu. Inaonekana*

*kama Bwana anajua kile Anachozungumzia, umeamini hilo? Kula kula ovyo siku nzima kunafanya viyeyusha chakula au 'enzymes' za kuyeyusha chakula zipate shida na hivyo kuvembewa tumbo, kuongeza uzito usio mzuri na kufanya mtu awe na tabia ya ulafi.*

**B. Usile kupita kiasi.**
"Weka kisu kooni, ikiwa wewe ni mtu wa kula." Mithali 23:2 . Katika Luka 21:34 , Kristo anaonya haswa dhidi ya "kula kupita kiasi" katika siku za mwisho. Ulafi au uchu wa chakula unahusika na magonjwa mengi ya mitindo ya maisha kama vile presha, moyo, unene uliopitiliza, nyongo, kisukari, baridi yabisi, magonjwa ya akili nk.

**C. Usiwe na wivu au kinyongo.**
Maovu haya hukinzana na michakato ya mwili. Biblia inasema kwamba wivu huleta "kuoza kwa mifupa." Mithali 14:30. Kristo anatuamuru tuondoe kinyongo ambacho wengine wanaweza kuwa nacho dhidi yetu ( Mathayo 5:23 , 24 ).

**D. Dumisha tabia ya uchangamfu na furaha.**

"Moyo uliochangamka hufanya kazi nzuri kama dawa." Mithali 17:22 . "Aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo." Mithali 23:7. Magonjwa mengi ambayo watu wanaugua ni matokeo ya akili kuathiriwa na misongo, huzuni, magonvi nk. Tabia ya uchangamfu, na furaha huleta afya na kuongeza maisha.

**E. Weka imani kamili kwa Bwana.**
"Kumcha Bwana huelekea uzima; Naye aliye nacho atakaa kuridhika." Mithali 19:23 . Kumtumaini Bwana huimarisha afya na uzima. "Mwanangu, sikiliza Maneno Yangu. ... Maana ni uhai kwa wale wayapatao, na afya ya mwili wao wote." Mithali 4:20-22 . Kwa hiyo afya inatokana na kutii amri za Mungu na kumtumaini kikamilifu.

**F. Sawazisha kazi (balansi) na mazoezi na kulala na kupumzika.**
"Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako; siku hiyo usifanye kazi yo yote." Kutoka 20:9 , 10 . "Usingizi wa mtenda kazi ni mtamu." Mhubiri 5:12. "Kwa jasho la uso wako utakula mkate." Mwanzo 3:19 . "Ni bure kwenu kuamka mapema, na kuchelewa kuketi." Zaburi 127:2 . "Kwa maana mwanadamu hupata nini katika kazi yake yote, na taabu ya moyo wake, anayoifanya chini ya jua? ... moyo wake hautulii usiku. Hayo nayo ni ubatili." Mhubiri 2:22 , 23 .

**G. Weka mwili wako safi.**
"Kuweni safi." Isaya 52:11 .

**H. Uwe na kiasi katika mambo yote.**
"Kila mtu ashindanaye ana kiasi katika mambo yote." 1 Wakorintho 9:25 . "Upole wenu na ujulikane kwa watu wote." Wafilipi 4:5 . Mkristo ataepuka kabisa mambo yote yenye madhara na atakuwa mwenye kiasi katika yale yaliyo mema, mfano chakula kizuri, kitatumiwa kwa kiasi, na yale yaliyo mabaya kama sigara, pombe, na kahawa atayaepuka kabisa, yaani hatayatumia hata kidogo. Tabia zinazoumiza afya huvunja amri "Usiue." Huua polepole. Zinaua mwili kwa taratibu.

**I. Epuka vichocheo vyote vyenye madhara.**
Hapa kuna mshangao kwa wengine. Sayansi ya tiba imethibitisha ukweli kwamba chai, kahawa, na vinywaji baridi ambavyo vina dawa ya kulevya ya kafeini na viambato vingine vyenye madhara vyote vinadhuru mwili wa binadamu (mfano ni seven up, cocacola, redbull na energy drink au vinywaji vya nishati). Hakuna kati ya hivi iliyo na lishe isipokuwa sukari au krimu iongezwe, na wengi wetu tayari tunatumia sukari nyingi hivyo tuviache. Vichocheo hutoa msisimko bandia na wenye hatari, na ni kama kujaribu kubeba tani moja ya mzigo kwenye toroli. Umaarufu wa vinywaji hautokani na ladha au matangazo ila kipimo cha kafeini kilichomo ndani, watu wanakuwa wamepata uraibu. Wamarekani wengi ni wagonjwa kwa sababu ya uraibu wao wa kahawa, chai nyeusi ya china, na vinywaji baridi vyenye kafeini. Lakini msiba halisi ni kwamba wanaume na wanawake wanaotafuta amani na nguvu wanatumia chai na kahawa kama mbadala wa gharama ndogo ukilinganisha na sala na mafunzo la Biblia. Hii inamfurahisha shetani na kuharibu maisha ya mwanadamu.

**J. Fanya wakati wa chakula uwe wa furaha.**
"Kila mtu ale na kunywa, na kujiburudisha katika mema ya kazi yake yote; hiyo ni zawadi ya Mungu." Mhubiri 3:13 . Matukio yasiyofurahisha wakati wa chakula huzuia usagaji chakula. Yaepuke. Angalia mtandano kitabu au muhtasari wa kitabu "Jinsi ya kuua familia yako kwa chakula na watu wasijue!" Inaelezea wapishi wengi hasa wakina mama wanavyoziua familia zao kwa upishi wao " ***"How to Kill Your Loved Ones With Food,*** **and get away with it" by Dr. Errol Stanford Ph.D., N.D.**

**K. Wasaidie wahitaji.**
"Vifungue vifungo vya uovu, ... ifungue mizigo mizito, ... uwapatie wenye njaa chakula chako, ... uwalete maskini waliotupwa nje nyumbani kwako ... uwaonapo walio uchi, .. .mfunike ... na afya yako itatokea upesi." Isaya 58:6-8 . Hili ni jambo la wazi sana kutoelewa: tunapowasaidia maskini na wahitaji, tunaboresha afya zetu wenyewe.
Kupuuza sheria za afya za Mungu ni njia ya uhakika ya kuishia kwenye upasuaji.

**11. Ni kumbukizi gani zito linalotolewa kwa wale wanaopuuza sheria za Mungu?**

"Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna." Wagalatia 6:7 .

**Jibu:** Jibu ni rahisi sana kukosea. Wale wanaovunja sheria za Mungu kuhusu utunzaji wa mashine ya mwili watavuna miili iliyovunjika na maisha yanayochosha mwili na kuufanya unyong'onyee (burnt bodies), kama vile mtu anayetumia gari lake vibaya, gari hilo litakuwa na shida kubwa. Na wale wanaoendelea kuvunja sheria za Mungu za afya hatimaye wataangamizwa na Bwana ( 1 Wakorintho 3:16 , 17 ). Sheria za afya za Mungu si za kiholela. Ni sheria za asili, zilizowekwa katika milki yote ya Mungu, kama sheria ya uvutano. Kupuuza sheria hizi daima huleta matokeo fulani mabaya. Biblia inasema, "Laana isiyo na sababu haitakuja." Mithali 26:2 . Shida inakuja tunapopuuza sheria za afya. Mungu, kwa rehema Zake nyingi, anatuambia

sheria hizi ni zipi ili tuepuke majanga yanayotokana na kuzivunja.

Wazazi wanaotumia dawa za kulevya mara nyingi husambaza udhaifu kwa watoto wao pia.

**12. Ni kweli gani yenye kuogopesha na kushtua kuhusu afya inayohusu watoto na wajukuu wetu?**

"Usiile, ili upate kufanikiwa wewe na watoto wako baada yako." Kumbukumbu la Torati 12:25 . "Mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu Mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao." Kutoka 20:5 .

**Jibu:** Mungu anaweka wazi kwamba watoto na wajukuu (hadi kizazi cha nne) hulipa ujinga wa wazazi wanaopuuza sheria za afya za Mungu.

Watoto na wajukuu hurithi miili iliyodhoofika, yenye magonjwa wakati mama na baba wanapoasi sheria za Mungu kwa maisha yao. Je, hivi ndivyo unavyotaka kwa watoto wako wapendwa na wajukuu? Cha kueleweka zaidi ni yale mazoea mabaya unayoyatenda, watoto wako wanayaona na kuyapeleka majumbani mwao wakiwa watu wazima wanapojitegemea. Mfano unapokula nafaka zilizokobolewa, unapotumia mafuta mengi kwenye kuunga mboga, unapotumia chumvi nyingi kwenye chakula, unapoacha kula matunda na mboga na kukazania nyama, unapokunywa soda, pombe na kadhalika, watoto wako wanakufuatiliza jinsi unavyofanya! Watoto wanajifunza kwa mfano mwenendo wa afya kuliko maneno ya mdomoni, wafundishe watoto kushugulikia chakula kwa hekima wakijali sheria za Mungu, lishe, ladha, gharama na upatikanaji pale unapoishi. Bila shaka afya inatunzwa kirahisi kwa kuwa na bustani ya mboga mwaka mzima nyumbani mwako, angalia zile mboga ambazo unaweza kuchuma kila siku na uzilime, kishe angalia nafaka bora, ukiwa na mboga nzuri, unachohitaji ni nafaka yenye lishe nzuri kama vile mtama, ulezi, uwele nk

Mazoezi yanayofanywa nje yatatusaidia kujiandaa kwa ajili ya mbinguni.

**13. Neno la Mungu hufunua jambo gani lenye kuogopesha na kuhuzunisha zaidi?**

"Hakitaingia humo chochote kilicho najisi. Ufunuo 21:27 . "Lakini wale ambao mioyo yao inaenda kuufuata moyo wa machukizo yao, na machukizo yao, nitaleta njia yao juu ya vichwa vyao wenyewe, asema Bwana MUNGU." Ezekieli 11:21 .

**Jibu:** Hakuna kitu kisicho kisafi au najisi kitakachoruhusiwa katika ufalme wa Mungu. Tabia zote chafu zinamtia mtu unajisi. Matumizi ya chakula kisichofaa humtia mtu unajisi (Danieli 1:8 ). Inatisha, lakini ni kweli. Kuchagua "njia zao wenyewe" na zile ambazo Mungu "hakupendezwa nazo" kutagharimu watu wokovu wao wa milele ( Isaya 66:3 , 4 , 15-17 ). Daniel angebugiabugia chakula chochote kwa ulafi angetekewa na uchawi wa Babeli, na asingeishi miaka zaidi ya 90 au hata kupewa njozi na ndoto na Bwana! Aliazimia moyoni mwake kwamba hatakula chakula cha mfalme chenye machukizo kwa Mungu. Je, unaazimia wewe moyoni mwako leo kutokula chakula ambacho Mungu amesema usile?

Wakristo wanyoofu, walio hai watataka kuleta maisha yao kupatana na sheria za afya za Mungu.

**14. Kila Mkristo mnyoofu anapaswa kujitahidi kufanya nini mara moja?**

"Na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho." 2 Wakorintho 7:1 . "Kila mtu aliye na tumaini hili ndani yake, anajitakasa, kama Yeye [Kristo] alivyo mtakatifu." 1 Yohana 3:3 . "Mkinipenda, mtazishika amri Zangu." Yohana 14:15 .

**Jibu:** Wakristo waaminifu wataleta maisha yao katika upatanifu na kanuni za Mungu mara moja, kwa sababu wanampenda Yeye. Wanajua kwamba sheria Zake huongeza sana furaha yao na kuwalinda kutokana na magonjwa ya shetani ( Matendo 10:38 ). Mashauri na sheria za Mungu ni kwa faida yetu sikuzote, kama vile sheria na mashauri ya wazazi yanavyowafaa watoto wao. Na tukishajua vyema, Mungu anatuwajibisha. "Kwake yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi." Yakobo 4:17 .

Mazoea mabaya yanayotufunga yanaweza kuvunjwa haraka na Yesu.

**15. Lakini nina wasiwasi kwa sababu baadhi ya tabia zangu mbaya zimenifunga kwa nguvu sana. Naweza kufanya nini?**

"Wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu." Yohana 1:12 . "Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu." Wafilipi 4:13 .

**Jibu:** Chukua tabia hizi zote kwa Kristo na uziweke miguuni Pake. Kwa furaha Yeye atakupa moyo mpya na uwezo unaohitaji ili kuvunja tabia yoyote mbaya na kuwa mwana au binti wa Mungu ( Ezekieli 11:18 , 19 ). Inafurahisha na kuchangamsha jinsi gani kujua kwamba "mambo yote yanawezekana kwa Mungu." Marko 10:27 . Na Yesu anasema, "Yeye ajaye Kwangu sitamtupa nje kamwe." Yohana 6:37 . Yesu Yuko tayari kuvunja pingu zilizotufunga, haijalishi ni ulafi, mazoea au uraibu wa aina gani. Anatamani kutuweka huru, na atafanya, ikiwa tu tutamruhusu. Wasiwasi wetu, tabia mbaya, mivutano ya neva za fahamu, na hofu zitatoweka tunapofanya agizo Lake. Anasema, "Hayo nimewaambia ... ili furaha yenu iwe kamili." Yohana 15:11 . Ibilisi anabishana kwamba uhuru unapatikana katika kutotii, lakini huu ni uongo ( Yohana 8:44 ).

Mbingu hazitakuwa na magonjwa na hitilafu zote za mwili. Wakaaji wake wote watafuata sheria za Mungu za uzima.

**16. Ni ahadi gani zenye kusisimua zinazotolewa kuhusu ufalme mpya wa Mungu?**

"Wala mwenyeji hatasema, Mimi mgonjwa." Isaya 33:24 . "Wala kifo hakitakuwapo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena." Ufunuo 21:4 . "Watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia." Isaya 40:31 .

**Jibu:** Raia wa ufalme mpya wa Mungu watatii sheria Zake za afya, na hakutakuwa na magonjwa wala unyonge wa aina yoyote. Watabarikiwa kwa nguvu na ujana wa milele na wataishi na Mungu katika shangwe na furaha kuu katika umilele wote.

**17. Kwa kuwa maisha yenye afya ni sehemu ya dini ya Biblia, ni mpango wangu kufuata kanuni za afya za Mungu.**

**Jibu:**

## MASWALI YA KUFIKIRIA NA KUCHEUA

**1. 1Timotheo 4:4 inasema, "Kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa." Je, unaweza kueleza hili?**

Kifungu hiki cha Maandiko (mstari wa 3) kinarejelea nyama "ambazo Mungu aliziumba ili zipokewe kwa shukrani" na watu Wake. Nyama hizi, kama tulivyokwisha gundua, ni zile nyama zilizo safi zilizoorodheshwa katika Mambo ya Walawi sura ya 11 na Kumbukumbu la Torati sura ya 14. Mstari wa 4 unaweka wazi kwamba viumbe vyote vya Mungu ni vyema na si vya kukataliwa, mradi tu wao ni miongoni mwa wale walioumbwa  "ili kupokelewa kwa shukrani" (wanyama walio safi). Mstari wa 5 unasema kwa nini wanyama hao (au vyakula) vinakubalika: "wanatakaswa" na Neno la Mungu, linalosema kuwa wao ni safi, na kwa "sala" ya baraka, ambayo hutolewa kabla ya mlo. Tafadhali kumbuka, hata hivyo, kwamba Mungu atawaangamiza watu wanaojaribu "kujitakasa" huku wakila vyakula najisi ( Isaya 66:17 ).

**2. Mathayo 15:11 inasema, "Si kile kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi, bali kile kitokacho." Je, unaelezaje hili?**

Somo katika Mathayo 15:1-20 ni kula bila kunawa mikono kwanza (mstari wa 2). Mtazamo sio kula, lakini kuosha. Waandishi walifundisha kwamba kula chakula chochote bila kuoshwa kwa *utaratibu maalum* kunamtia unajisi mlaji. Yesu alisema uoshaji wa kiibada haukuwa na maana. Katika mstari wa 19, aliorodhesha maovu fulani--mauaji, uzinzi, wizi n.k. Kisha akamalizia, "Haya ndiyo yamtiayo mtu unajisi; lakini kula bila kunawa mikono hakumtii mtu unajisi." Kifungu cha 20.

**3. Lakini je, Yesu hakuwasafisha wanyama wote katika maono ya Petro, kama ilivyorekodiwa katika Matendo 10?**

Hapana! Kwa kweli, mada ya maono haya sio wanyama, lakini watu. Mungu alimpa Petro maono haya ili kumwonyesha kwamba watu wa mataifa mengine hawakuwa najisi, kama Wayahudi walivyoamini. Mungu alikuwa amemwagiza Kornelio, mtu wa Mataifa, kutuma watu kumtembelea Petro. Lakini Petro angekataa kuwaona kama Mungu hangempa maono haya, kwa sababu sheria ya Kiyahudi ilikataza kuwakaribisha watu wa mataifa mengine (mstari wa 28). Lakini watu hao walipofika, Petro aliwakaribisha, akieleza kwamba kwa kawaida hangefanya hivyo, lakini "Mungu amenionyesha nisimwite mtu awaye yote najisi au najisi. Mstari wa 28. Katika sura iliyofuata (Matendo 11), washiriki wa kanisa walimkosoa Petro kwa kuzungumza na hawa watu wa mataifa. Kwa hiyo Petro aliwaambia kisa chote cha maono yake na maana yake. Na Matendo 11:18 inasema, "Waliposikia hayo wakanyamaza, wakamtukuza Mungu, wakisema, Basi, Mungu amewajalia hata Mataifa nao toba liletalo uzima.

**4. Mungu alimwumba nguruwe kwa ajili ya nini, ikiwa sio kula?**

Mungu aliumba hawa wanyama wasife milele! Ila baada ya kifo kazi au kusudi la nguruwe likawa kama alivyomwumba tai au kaa/kamba--kula mizoga au kuzoa takataka na kusafisha mazingira! Na nguruwe hutumikia kwa kusudi hili jinsi ya ajabu. Sasa baada ua wanyama hawa kusafisha mazingira kwa kula mizoga, kwanini sisi tuwale na kupakia mizoga mibaya hii matumboni mwetu?

**5. Warumi 14:3, 14, 20 husema: "Yeye asiyekula na asimhukumu yeye alaye. "Hakuna kitu najisi chenyewe." "Vitu vyote ni safi." Je, unaweza kueleza hili?**

Mstari wa 3 hadi 6 ni mjadala wa wale wanaokula vitu fulani dhidi ya wale wasiokula. Kifungu hakisemi kama ni sawa, lakini badala yake kinashauri kwamba watu wasitoe hukumu kwa wengine. Badala yake, acha Mungu awe Mwamuzi (mistari 4,10-12). Mistari ya 14 na 20 inarejelea vyakula ambavyo vilitolewa mara ya kwanza kwa sanamu (na hivyo vilikuwa najisi kiibada)—sio nyama safi na najisi za Mambo ya Walawi sura ya 11. (Soma 1 Wakorintho 8: 1 , 4 , 10 , 13 ). Jambo la mjadala ni kwamba hakuna chakula ambacho ni "najisi" au si "najisi" kwa sababu tu kimetolewa kwa sanamu, kwa sababu sanamu "si kitu duniani." 1 Wakorintho 8:4 . Lakini ikiwa dhamiri ya mtu inamsumbua kwa kula chakula hicho, basi anapaswa kukiacha. Au hata ikiwa kula kwake kunamuudhi ndugu, anapaswa kujiepusha vivyo hivyo.

**6. Je, sheria za afya na kula na kunywa ni muhimu kwangu binafsi? Ikiwa ninampenda Bwana, je, hiyo haitoshi?**

Ni suala la uzima na kifo, kwa sababu sheria hizi zinahusisha utii. "Yeye Amekuwa chanzo cha wokovu wa milele kwa wote wanaomtii." Waebrania 5:9 . "Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni." Mathayo 7:21 . Upendo kwa Kristo unahusika hapa kwa sababu anasema, "Mkinipenda, mtazishika amri Zangu." Yohana 14:15 . Tunapompenda Bwana kweli, tutamtii kwa furaha bila kukwepa au kutoa visingizio. Huu ni mtihani mkuu. Kipimo kizito!

## MASWALI YA CHEMSHA BONGO AU KWIZZ

**1. Kufuata kanuni za afya za Mungu kwa mwili wa mwanadamu (1)**

_____ Ni muhimu kwa watoto, lakini sio muhimu sana kwa mtu mzima.
_____ Ni sehemu muhimu sana ya dini ya Kweli ya Biblia.
_____ Haina uhusiano wowote na dini ya mtu.

**2. Sheria za afya za Mungu zilitolewa (1)**

_____ Na Mungu mwenye upendo aliyetuumba hapo mwanzo, Naye anajua ni nini kilicho bora zaidi kwa furaha yetu.
_____ Kwa Wayahudi pekee na haitumiki leo.
_____ Ili kutuonyesha Yeye ni bosi na anaweza kututawala.

**3. Mkristo wa kweli ata (1)**
_____ Kula na kunywa chochote anachotamani.
_____ Mpenda tu Bwana sana na kupuuza sheria Zake za afya kwa sababu ziliondolewa msalabani.
_______ Kula na kunywa vile tu vitu ambavyo vitaimarisha mwili, akili, na tabia na kuleta heshima kwa Mungu.

**4. Lishe ya kwanza ya mwanadamu (1)**
_____ Ilijumuisha matunda, nafaka, na karanga.
_____ Ilijumuisha vileo na vyakula vya nyama.
_____ Ilijumuisha chochote na kila kitu ambacho Adamu na Hawa walitaka kula.

**5. Mungu anaorodhesha viumbe hawa kuwa najisi: (7)**
_____ Ng'ombe.
_____ Nguruwe.
_____ Kuku.
_____ Kuchakulo.
_____ Sungura.
_____ Kambare.
_____ Kulungu.
_____ Panya.
_____ Twiga.
_____ Kamba.
_____ Kamba.
_____ Mbuzi.

**6. Vinywaji vyenye kileo ni (1)**
_____ Ni sawa kwa Mkristo vikitumiwa kwa kiasi.
_____ Sio sahihi kwa mtu kutumia endapo mtu anadhani kuwa asivitumie.
_____ Havipaswi kutumiwa na Mkristo.

**7. Matumizi ya tumbaku ni (1)**
_____ Shuguli binafsi ya mtu, haina uhusiano wowote na dini yake.
_____ Ni dhambi, na Mkristo hataitumia kwa namna yoyote.
_____ Inasaidia kikohozi na Mkristo atumie kama dawa.

**8. Angalia sheria za afya zilizoorodheshwa hapa chini ambazo ndiyo sheria za afya za Mungu: (9)**
_____ Usile kupita kiasi.
_____ Vuta sigara mbili baada ya kila mlo.
_____ Kuwa na furaha na uchangamfu.
_____ Kunywa pombe kabla ya kwenda kulala.
_____ Weka mwili wako safi.
_____ Kula nyama ya nguruwe kwa wingi.
_____ Kunywa kahawa na chai nyeusi ya china kwa wingi.
_______Uwe na kiasi katika mambo yote.
_____ Kula milo kwa vipindi vinavyoachanisha masaa ili tumbo lipumzike.
_____ Usiwe na kinyongo.

_____ Sawazisha kazi, mazoezi, na usingizi.
_____ Mtumaini Bwana kikamilifu.
_____ Usitumie mafuta na damu ya wanyama.

**9. Ukweli muhimu sana kuhusu sheria za afya za Mungu ni kwamba (1)**
_____ Watoto na wajukuu mara nyingi wana miili na akili dhaifu kwa sababu wazazi hupuuza sheria za afya za Mungu.
_____ Sheria hizi zilikuwa kwa ajili ya Wayahudi pekee na hazitumiki leo.
_____ Kama kweli tunapompenda Kristo, sheria Zake za afya si muhimu.

**10. Njia bora ya kushinda mazoea ya dhambi ni (1)**
_____ 'Kupunguza.' hizo dhambi kama kunywa pombe nusu glasi tu
_______ Kujikabidhi kikamilifu kwa Kristo, anayetupa uwezo wa kufanya mambo yote.
_____ Kutumiani kwamba mazoea hayo yataondoka yenyewe.

**11. Sheria za Mungu za afya ni (1)**
_____ Kama kanuni za kuendesha gari: Ni bora kwetu, na tunaingia kwenye matatizo makubwa tunapozipuuza.
_____ Sehemu ya sheria ya Musa ambazo ziliondolewa pale msalabani.
_____ Wazo zuri, lakini haliathiri uhusiano wa mtu na Mungu.

**12. Mkristo mwaminifu (2)**

_____ Atatumia muda mwingi kusali na kupuuza sheria za afya za Mungu.

_____ Atabadilisha mara moja tabia yoyote anapoiona inakinzana na kanuni za Mungu, kwa sababu tunapompenda Kristo sisi tutashika sheria na amri Zake kwa furaha.

_____ Atajisikia huru kutumia tumbaku.

_____Atajua sheria za Mungu za afya zinashugulika na kuzuia magonjwa zaidi ya kuponya

## Je, Utiifu ni kuwa mfarisayo au kuwa shupavu wa sheria (legalism)?

## Somo la 14

Watu wanaweza kuhisi kwamba wanaweza kuepuka adhabu kwa kukiuka sheria ya trafiki au kudanganya kodi zao, lakini Mungu na sheria Zake hufanya kazi kwa njia tofauti zaidi na wanadamu. Mungu huona kila kitu tunachofanya, anasikia kila kitu tunachosema, na anajali sana jinsi tunavyotenda yaani nia zetu na mielekeo yetu. Ingawa Mwenyezi Mungu hutoa msamaha kwa dhambi zetu, bado kuna matokeo mabaya ya kuivunja sheria ya Mungu. cha kushangaza ni kuwa baadhi ya Wakristo wanasema jaribio lolote la kutii sheria ya Mungu ni sawa na kuwa mfarisayo (legalism) . Lakini Yesu alisema ikiwa unampenda Mungu kweli, utafanya kile anachokuomba ukifanye. Je, ni kweli kwamba utiifu wa sheria ni kuwa mfarisayo au kupitiliza kwa kuishika sheria mpaka mtu anakuwa mnafiki au mkavu/

baridi kwa huruma zake (legalism)? Chukua muda kusoma Mwongozo huu kwa makini... matokeo ya milele yamo hatarini tusipoelewa somo hili vizuri!
Mungu anakujua na kukujali wewe binafsi.

**1. Je, ni kweli Mungu ananiona na kunijali mimi binafsi?**

"Wewe Mungu unaniona." Mwanzo 16:13 . "Ee Bwana, umenichunguza na kunijua. Wewe wajua kuketi kwangu na kuamka kwangu, unaelewa mawazo yangu tokea mbali. Wewe ... unazifahamu njia zangu zote. Maana hamna neno ulimini mwangu, ila , tazama, Ee Bwana, Wewe wajua kabisa." Zaburi 139:1-4 . "Lakini hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote." Luka 12:7 .

**Jibu:** Ndiyo, Mungu anamjua kila mmoja wetu (kila mtu duniani) kuliko tunavyojijua sisi wenyewe. Anapendezwa kibinafsi na kila mwanadamu na hutazama kwa uangalifu yote tunayofanya. Hakuna neno, wazo, au tendo moja ambalo limefichwa Kwake.

Tafuta katika Biblia ili upate mapenzi ya Mungu. Ni usalama wako pekee.

**2. Je, ninaweza kuokolewa katika ufalme Wake bila kutii Neno Lake, kama linavyopatikana katika Biblia Takatifu?**

"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni." Mathayo 7:21 . "Ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri." Mathayo 19:17 . "Amekuwa chanzo cha wokovu wa milele kwa wote wanaomtii." Waebrania 5:9 .

**Jibu:** Hapana! Maandiko yako wazi sana juu ya jambo hili. Wokovu na ufalme wa mbinguni ni kwa wale wanaotii amri za Bwana. Mungu haahidi uzima wa milele kwa wale wanaokiri imani kwa mdomo tu hata kama ni washiriki wa kanisa au wamebatizwa, bali kwa wale wanaofanya mapenzi Yake, ambayo yamefunuliwa katika Maandiko. Bila shaka, utii huu unawezekana kupitia Kristo pekee ( Matendo 4:12 ).

Kuna Njia moja tu inayoongoza mbinguni. Biblia ndiyo ramani inayotuonyesha njia.

**3. Kwa nini Mungu anahitaji utii? Kwa nini ni lazima?**

"Kwa sababu mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache." Mathayo 7:14 . "Bali anitendaye dhambi hujidhulumu nafsi yake mwenyewe; wote wanichukiao hupenda mauti." Mithali 8:36 . "BWANA akatuamuru kuzifanya amri hizi zote, tumche Bwana, Mungu wetu, kwa wema wetu siku zote, ili atuhifadhi hai." Kumbukumbu la Torati 6:24 .

**Jibu:** Kwa sababu kuna njia moja tu nyembamba iendayo kwenye kumcha Mungu, na hivyo kwenye ufalme Wake. **Barabara zote hazielekei mahali pamoja, yaani barabara zote hazielekei mbinguni, alimradi uko kwenye dini fulani.** Biblia ndiyo ramani na kitabu cha mwongozo chenye maagizo kamili kuliko vyote duniani, ndicho kitabu PEKEE chenye Historia ya Mwanadamu kuanzia mwanzo mpaka mwisho kwa Ukweli ote. Ndiyo Mwongozo pekee wenye maonyo, na taarifa

kuhusu jinsi ya kuufikia ufalme huo kwa usalama. Kupuuza sehemu yoyote yake, kunamwelekeza mwanadamu mbali na Mungu na ufalme Wake. Ulimwengu wa Mungu ni ulimwengu wa sheria na utaratibu. Sheria za asili, za kiadili, na za kiroho zinahusika. Kuvunja yoyote ya sheria hizi daima kuna matokeo fulani ya kudumu. Kama Biblia haikutolewa, watu wangegundua mapema au baadaye (kwa majaribio na makosa) kwamba kanuni kuu za Biblia zipo na ni za Kweli.

Kanuni hizi za Biblia zimeandikwa katika mifumo yetu ya fahamu au neva, tezi, na akili. Zinapopuuzwa, basi mishipa iliyovunjika hutokeza, magonjwa, na kukosa furaha kwa kila namna. Kwa hiyo maneno ya Biblia si ushauri tu ambao tunaweza kuukubali au kuupuuza bila matokeo au jinsi tutakavyo, au pale tunapojisikia. Biblia inaeleza matokeo hayo na kueleza jinsi ya kuyaepuka. Mtu hawezi kuishi jinsi apendavyo na bado akawa kama kimungu hivi kama vile mjenzi asivyoweza kupuuza ramani za nyumba bila kupatwa na matatizo. Hii ndiyo sababu Mungu anauliza wote kufuata mpango wa Maandiko Matakatifu. Hakuna njia nyingine ya kuwa kama Yeye au kufanana na Yeye na hivyo kufaa kwa ajili ya nafasi katika ufalme Wake. Na hakuna njia nyingine ya kupata furaha ya Kweli.

Dhambi inaweza kuharibiwa na Mungu kwa usalama tu baada ya watu wote kuelewa na kukiri kwamba Yeye ni mwenye haki, mwenye upendo, na mwenye huruma.

**4. Kwa nini Mungu anaruhusu kutotii kuendelee? Kwa nini asiharibu dhambi na wenye dhambi sasa hivi bila ya kuchelewa?**

"Tazama, Bwana anakuja na watakatifu Wake elfu kumi, ili kuwahukumu watu wote, na kuwaadhibu wote wasiomcha Mungu kati yao kwa ajili ya matendo yao yote ya uasi waliyoyatenda, na maneno magumu waliyoyanena wenye dhambi wasiomcha Mungu. dhidi yake." Yuda 14 , 15 . "Kama niishivyo, asema Bwana, kila goti litapigwa mbele Zangu, na kila ulimi utakiri kwa Mungu." Warumi 14:11 .

**Jibu:** Mungu anaruhusu kutotii na dhambi kuendelea hadi watu wote kila mahali watakaposadikishwa kikamili kuhusu haki, upendo, na rehema ya Mungu. Wote hatimaye watatambua kwamba Mungu, kwa kuhitaji utii, hajaribu kulazimisha mapenzi Yake juu yetu, bali Yeye anajaribu kutuzuia tusijidhuru na kujiangamiza wenyewe. Tatizo la dhambi halitatuliwi mpaka hata wale wenye dhambi walio na dharau na wagumu wasadikishwe juu ya upendo wa Mungu na kukiri kwamba Yeye ni mwenye haki. Itachukua labda janga kubwa au baya zaidi kuwashawishi wengine, lakini matokeo ya kutisha ya maisha ya dhambi hatimaye yatasadikisha wote kwamba Mungu ni wa haki na sahihi. Nawe ni shahidi kwamba kuna wakati umetenda dhambi na ulikuwa gizani, na kwamba tunakumbushwa kwenye Waefeso 2:8 kwamba kama Mungu angeyahesabu makosa yetu binadamu, ni nani kweli angesimama, lakini kuna kusamehewa Naye, kunakoendelea kila siku maishani mwetu!

Ndipo hapo, na ndipo tu, dhambi na kutotii vinaweza kukomeshwa kwa usalama na Bwana.

Wote wanaochagua kutomfuata Kristo kwa kujua hatimaye wataangamizwa na dhambi wanayoipenda.

**5. Je, kweli Mungu atawaangamiza wasiotii?**

"Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa kuzimu, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu. 2 Petro 2:4 . "Waovu wote atawaangamiza." Zaburi 145:20 . "katika mwali wa moto akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo." 2 Wathesalonike 1:8 .

**Jibu:** Hakuna swali au shaka juu ya jambo hili. Waasi, akiwemo ndani Ibilisi na malaika zake waliotenda dhambi, wataangamizwa. Hii ikiwa ni kweli, kwa hakika ni wakati mwafaka wa kuachana na mambo yote ya kizunguzungu cha dhambi kuhusu ni nini kilicho sahihi au kilicho dhambi. Ni afadhali watu waache kuruhusu mawazo yao ya kipumbavu na mawazo ya kujikweza kuwaongoza na kuzingatia kitabu kikuu cha Mungu. Na bora wafanye sasa - hakuna wakati mwingi uliobaki!

Mungu anaahidi kwamba nikitafuta Neno Lake kwa ukweli na kulifuata kwa dhati, sitaishia katika makosa.

**6. Ninataka kutii sheria zote za Mungu. Ninawezaje kuwa na hakika kwamba sitapuuza hata moja?**

"Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata." Mathayo 7:7 . "Jifunze kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, ... ukitumia kwa halali Neno la kweli." 2 Timotheo 2:15 . "Mtu akipenda kuyafanya mapenzi Yake, atajua habari ya yale mafundisho kwamba yanatoka kwa Mungu." Yohana 7:17 . "Enendeni maadamu mnayo nuru, giza lisije likawapata." Yohana 12:35 . "Mara tu watakaposikia habari Zangu, watanitii." Zaburi 18:44 .

**Jibu:** Mungu haachi nafasi ya shaka. Anaahidi kuniepusha na makosa na kuniongoza salama kwenye Kweli yote ikiwa mimi: (1) nitasali kwa bidii ili kupata mwongozo, (2) Nitajifunza Neno la Mungu kwa unyoofu, na (3) Nitafuata Kweli mara tu ninapoonyeshwa.

Kucheza mbuni katika mambo ya kiroho huleta maafa na uharibifu.

**7. Je, Mungu ananihesabu kuwa na hatia kwa kutotii Kweli ya Biblia ambayo sijapata kuwekwa wazi kamwe?**

"Kama mngekuwa vipofu, hamngekuwa na dhambi; lakini sasa mwasema, Tunaona; basi dhambi yenu inakaa." Yohana 9:41 . "Kwake yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi." Yakobo 4:17 . "Watu Wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, Mimi Nami nitakukataa wewe." Hosea 4:6 . "Tafuteni, nanyi mtapata." Mathayo 7:7 .

**Jibu:** Ikiwa sijapata nafasi ya kujifunza Kweli fulani ya Biblia, Mungu hanihesabii hatia. Lakini Biblia inafundisha kwamba ninawajibika kwa Mungu kwa nuru yote (maarifa ya haki) niliyo nayo na yote ninayoweza kuwa nayo! Hii inanibidisha kusoma ili nisiwe mjinga wa Maandiko.Watu wengi wanaokataa au kupuuza kusoma, kutafuta, kujifunza, na kusikiliza wataangamizwa na Mungu kwa sababu "wamekataa maarifa." Kucheza mchezo wa mbuni kwa kuficha kichwa mchangani, kwamba eti huonekani, na kumbe umbo lote lako liko wazi kabisa, ni katika mambo

haya muhimu tunayozungumzia kwamba ni mabaya kuyafanya. Ni jukumu langu kuuwinda/kuutafuta Ukweli kwa bidii.

Ni wawili tu kati ya maelfu ya Waisraeli waliotoka Misri walimfuata Mungu kikamilifu na kuweza kuingia katika nchi ya ahadi ya Kanaani.

**8. Je, Mungu hajali sana kuhusu utii kwa kila jambo na kwa mambo madogo-madogo, au sivyo?**

"Hakika hapana hata mmoja wa watu hao waliokwea kutoka Misri… atakayeiona hiyo nchi... kwa sababu hawakunifuata Mimi kabisa: isipokuwa Kalebu… na Yoshua… Hesabu 32:11 , 12 . "Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Mathayo 4:4 . "Ninyi mmekuwa rafiki Zangu, mkitenda niwaamuruyo." Yohana 15:14 .

**Jibu:** Hakika Yeye ni mahususi. Watu wa Mungu katika nyakati za Agano la Kale walijifunza hili kwa njia ngumu. Wale waliotoka Misri kwenda nchi ya ahadi ya Kanaani walikuwa 603,550 kwa idadi. Kati ya kundi hili, ni wawili tu (Kalebu na Yoshua) walimfuata Bwana kikamilifu, na wao peke yao waliingia Kanaani. Wale wengine 603,548 walikufa nyikani ikiwemo na Musa. Yesu anasema tunapaswa kuishi kwa "kila Neno" la Biblia. Hakuna Neno ambalo ndilo kubwa sana au Neno moja ambalo ni dogo sana. Yote ni muhimu.

Isipokuwa nifuate nuru mara tu inapofichuliwa, hatimaye hugeuka kuwa giza.

**9. Ninapogundua uYweli mpya, mimi husubiri hadi vikwazo vyote viondolewe kabla ya kuukumbatia. Je, jambo hili ni bora, au sivyo?**

"Enendeni maadamu mnayo nuru, giza lisije likawapata." Yohana 12:35 . "Nilifanya haraka, wala sikukawia kuyashika maagizo Yako." Zaburi 119:60 . Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa." Mathayo 6:33 . "Mara wanisikiapo watanitii." Zaburi 18:44 .

**Jibu:** Hapana, ukishaelewa Ukweli wa Biblia, sio bora kungoja. Kwa hakika, kuahirisha mambo ni mtego hatari sana wa shetani. Inaweza kuonekana kuwa si hatari sana kungoja, lakini Biblia inafundisha kwamba mtu asipochukua hatua mara moja juu ya nuru, inakuwa giza haraka. Vizuizi vya utii haviondolewi tunaposimama na kusubiri; badala yake, kwa kawaida huongezeka kwa ukubwa. Mwanadamu anamwambia Mungu, "Fungua njia, nami nitaenda mbele." Lakini njia ya Mungu ni kinyume kabisa. Anasema, "Songa mbele, Nami nitafungua njia."

Shetani alibuni uwongo kwamba utii hauwezekani.

**10. Lakini je, utii kamili si ni jambo lisilowezekana kwa mwanadamu?**

"Kwa Mungu yote yanawezekana." Mathayo 19:26 . "Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu." Wafilipi 4:13 . "Basi Mungu na ashukuriwe, atushangiliaye sikuzote katika Kristo." 2 Wakorintho 2:14 . "Akaaye ndani Yangu, Nami ndani yake, ... huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote." Yohana 15:5 . "Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi." Isaya 1:19 .

**Jibu:** Hakuna hata mmoja wetu anayeweza kutii kwa uwezo wake mwenyewe,

lakini kupitia Kristo tunaweza na lazima. Shetani, ili kufanya maombi ya Mungu yaonekane kuwa hayana akili, alibuni uongo kwamba utii hauwezekani.

Nikipuuza maonyo ya upendo ya Mungu, nitaangamia.

**11. Ni nini kitakachompata mtu ambaye kwa makusudi na akijua anaendelea na safari ya kutotii?**

"Tukitenda dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kKeli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha na ukali wa moto utakaowala wao wapingao." Waebrania 10:26 , 27 . "Enendeni maadamu mnayo nuru, giza lisije likawapata; kwa maana yeye aendaye gizani hajui aendako." Yohana 12:35 .

**Jibu:** Biblia haiachi nafasi ya shaka. Jibu ni la kustaajabisha na la kushtua, lakini ni Kweli. Mtu anapoikataa nuru kwa kujua na kuendelea kutotii, hatimaye nuru hiyo huzimika, na kuachwa katika giza kuu. Mtu anayekataa Ukweli hupokea "udanganyifu mkubwa" wa kuamini kwamba uongo ni Ukweli ( 2 Wathesalonike 2:11 ). Wakati hii inatokea, yeye anapotea kutoka wakati huo.

Hakuna mtoto atakayetii wazazi wake kikamilifu isipokuwa anawapenda.

**12. Nilifikiri upendo ulikuwa muhimu zaidi kuliko utii. Sivyo?**

"Yesu akajibu ... Mtu akinipenda, atayashika Maneno Yangu. ... Yeye asiyenipenda hayashiki Maneno Yangu." Yohana 14:23 , 24 . "Huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri Zake; na amri Zake si nzito." 1 Yohana 5:3 .

**Jibu:** Hapana, hata kidogo, jambo hilo si kweli! Biblia inafundisha kwamba upendo wa Kweli kwa Mungu hauwezi kuwepo bila utii. Wala mtu hawezi kuwa mtiifu kikweli bila upendo. Hakuna mtoto atakayewatii wazazi wake kikamili isipokuwa akiwapenda, wala hatawapenda wazazi wake ikiwa hatatii. Upendo wa kweli na utiifu ni kama mapacha waliozaliwa wakiwa wameshikana pamoja (siamese), Wanapotenganishwa, hufa.

Ni raia tu anayetii sheria ana uhuru. Vivyo hivyo, uhuru wa kweli wa Kikristo unamaanisha uhuru kutoka kwa kutotii.

**13. Lakini siku zote nilifikiri kwamba uhuru wa Kweli katika Kristo ulinifungua kutoka kwa utii. Sivyo?**

"Ninyi mkikaa katika Neno Langu, ... mtaifahamu Kweli, nayo hiyo Kweli itawaweka huru." "Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi." Yohana 8:31 , 32 , 34 . "Lakini Mungu na ashukuriwe kwa kuwa mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mmetii kwa mioyo yenu ile namna ya mafundisho ambayo mliwekwa chini yake. Basi, mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki." Waroma 6:17 , 18 . "Basi nitaishika sheria Yako sikuzote hata milele na milele. Nami nitakwenda mahali palipo huru, kwa maana nimetafuta mausia Yako." Zaburi 119:44 , 45 .

**Jibu:** Hapana. Uhuru wa Kweli unakuja tu kwa utii. Inamaanisha uhuru "kutoka kwa dhambi" ( Warumi 6:18 ), au kutotii, ambako ni kuvunja sheria ya Mungu ( 1 Yohana 3:4 ). Raia wanaotii sheria wana uhuru. Waasi wanakamatwa na kupoteza uhuru wao. Uhuru bila utii ni kama uhuru wa uongo wa puto linalopeperuka na kujiendea linapotaka au gari lisilo na dereva. Jambo linasababisha kuchanganyikiwa na machafuko. Uhuru wa Kweli wa Kikristo unamaanisha uhuru kutoka wa kukimbia kutotii. Kutotii siku zote huumiza mtu na kupelekea katika utumwa wenye ukatili wa shetani.

Watoto wenye upendo huwatii wazazi wao ingawa huenda wasielewe sikuzote ombi lao. Ndivyo ilivyo kwa watoto wa Mungu.

**14. Ninapoamini kwamba Mungu anahitaji jambo fulani, je, ni lazima nitii ingawa sielewi ni kwa nini analihitaji?**

"Nakusihi, uitii sauti ya Bwana ... ndivyo utakavyofanikiwa, na nafsi yako itaishi." Yeremia 38:20 . "Anayeutumainia moyo wake ni mpumbavu." Mithali 28:26 . "Heri kumtumaini Bwana kuliko kumtumaini mwanadamu." Zaburi 118:8 . "Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia Zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo Yangu kuliko mawazo yenu." Isaya 55:9 . Hukumu Zake hazichunguziki jinsi gani, na njia Zake hazitafutikani! Maana ni nani aliyeijua nia ya Bwana? Waroma 11:33 , 34 . "Nitawaongoza katika njia wasiyoijua." Isaya 42:16 . "Utanionyesha njia ya uzima." Zaburi 16:11 .

**Jibu:** Bila shaka! Ni lazima tumpe Mungu sifa ya hekima kiasi cha kutosha na hivyo Yeye anapotuambia jambo fulani katika hekima Yake, Yeye ameona mambo ambayo huenda sisi hatuyaelewi. Watoto wema huwatii wazazi wao hata kama sababu za amri zao haziko wazi. Imani sahili na tumaini katika Mungu vitatufanya tuamini kwamba Yeye anajua kilicho bora kwetu na hatawahi kutuongoza katika njia yoyote mbaya. Ni upumbavu kwetu, na upumbu kwetu, kuhoji uongozi wa Mungu, hata ule wakati ambao hatuelewi kabisa sababu Zake zote.

Ibilisi anataka umwasi Mungu kwa sababu anakuchukia na anataka upotee.

**15. Ni nani hasa anayesababisha kutotii, na kwa nini?**

"Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa maana Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo." "Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa Ibilisi; kila mtu asiyetenda haki hatokani na Mungu." 1 Yohana 3:8 , 10 . Shetani ... audanganyaye ulimwengu wote." Ufunuo 12:9 .

**Jibu:** Ibilisi anahusika. Anajua kwamba kutotii kote ni dhambi na kwamba dhambi huleta ukosefu wa furaha, misiba, kutengwa na Mungu, na hatimaye uharibifu. Kwa chuki kali Shetani anajaribu sana kumwongoza kila mtu kwenye uasi. Unahusika na uovu. Lazima ukabiliane na Ukweli na ufanye uamuzi kwa kusimama dede. Amua bila kuchukulia mambo lelemama, kwamba wewe utaacha kutii na kupotea, au utamkubali Kristo na kumtii na kuokolewa. Uamuzi wako kuhusu utii ni uamuzi kuhusu Kristo. Huwezi kumtenganisha Yeye na Kweli, kwa sababu anasema, "Mimi ni ... Kweli." Yohana 14:6 . "Chagueni hivi leo mtakayemtumikia." Yoshua 24:15 .

Kufuatia muujiza wa kuzaliwa upya (kubadilika), Mungu anaendelea kufanya miujiza ili kutuletea ukuaji wa Kikristo.

**16. Ni ahadi gani tukufu kuhusu muujiza mkuu zaidi ambayo Biblia huwapa watoto wa Mungu?**

"Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu." Wafilipi 1:6 .

**Jibu:** Mungu asifiwe! Anaahidi kwamba kama vile alivyofanya muujiza ili kutuletea kuzaliwa upya, Yeye pia ataendelea kufanya miujiza inayohitajika katika maisha yetu (tunapomfuata Yeye kwa furaha) hadi tutakapokuwa salama katika ufalme Wake.

**17. Inaniletea furaha kujua kwamba Yesu hatoi tu kuzaliwa upya kwa wale wanaomkubali na kumfuata, bali pia anaendelea kufanya miujiza inayohitajika katika maisha yao hadi wawe salama katika ufalme Wake. Yeye ni Mtakasaji, na Mwewezeshaji katika kukufikisha mbinguni salama, ana nguvu zote na maarifa yote kufanya hivyo, mimi na wewe hatuna nguvu wala maarifa. Mimi Ninataka kuanza kumtii kwa upendo na kumfuata Mwenyezi Mungu kikamilifu mara moja.**

**Jibu Lako ni nini, Liandike hapa:**

## MASWALI YA KUCHEUA NA KUFIKIRI

**1. Je, kuna yeyote atakayepotea ambaye anafikiri Kweli kwamba ameokoka?**

Ndiyo! Mathayo 7:21-23 inaweka wazi kwamba wengi wanaotabiri, kutoa pepo, na kufanya kazi nyingi za ajabu katika jina la Kristo watapotea lakini watafikiri wameokoka. Kristo alisema wamepotea kwa sababu hawakufanya "mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni." Mstari wa 21. Wale wanaokataa kumtii Mungu wataishia kuamini uongo ( 2 Wathesalonike 2:11 , 12 ) na hivyo kufikiri kwamba wameokolewa wakati badala yake wamepotea.

**2. Kwa kuwa kuna njia moja tu iliyo sawa, ni nini kitakachowapata watu wanyoofu wanaofikiri kikweli kuwa wako sahihi wakati wamekosea?**

Yesu anasema kwamba atawaita kwenye njia Yake ya Kweli, na kondoo Wake wa Kweli watasikia na kufuata ( Yohana 10:16 , 27 ).

**3. Je, uaminifu na bidii havitoshi?**

Hapana! Lazima pia tuwe sawa na Maandiko. Mtume Paulo alikuwa mwaminifu na mwenye bidii alipowatesa Wakristo kabla ya kuongoka kwake, lakini pia alikuwa katika makosa makubwa ( Matendo 22:3 , 4 ; 26:9-11 ).

**4. Je, ni jambo linalowezekana kisayansi kweli kwamba ungu anaweza kuona kila mtu kwa wakati mmoja?**

Ndivyo ilivyokuwa Gharika ya Nuhu (haikuwa na mvua kabla ya kunyesha-- Mwanzo 2:5 , 6 ), lakini ilitokea hata hivyo. Kujidai au kujifikiria kwamba wao ni "wanasayansi mashuhuri" na hivyo kutotii, ndilo jambo lilipendwa toka zamani na vizazi vyote, kuanzia Hawa, maana inafurahisha moyo wenye dhambi, angalia warumi Warumi 1:22 , ambao "wakijidai kuwa wenye hekima, wakawa wapumbavu."

**5. Nini kitatokea kwa watu ambao hawajapokea nuru?**

Biblia inasema kwamba wote wamepokea nuru fulani. Yeye "Ndiyo Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, ajaye katika ulimwengu. Yohana 1:9 . Kila mtu atahukumiwa kulingana na jinsi anavyofuata nuru inayopatikana. Hata wapagani wana nuru fulani na wanafuata sheria, kulingana na Warumi 2:14 , 15 .

**6. Nimemwomba Mungu anipe ishara ikiwa anataka nitii au nisitii. Hii ni salama, au sivyo?**

Hapana! Sio salama. Yesu alisema, "Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara. Mathayo 12:39 . Mafundisho yote yanapaswa kuchunguzwa na kupimwa na Biblia, na ikiwa yanapatana na Neno la Mungu, yanapaswa kukubaliwa na kufuatwa ( Isaya 8:20 ; 2 Timotheo 2:15 ). Watu ambao hawatakubali mafundisho yaliyo wazi ya Biblia hawangesadikishwa na ishara pia yaani hata miujiza ya kuhamisha milima itokee, haitawasaidia ng'o! Kama Yesu alivyosema, "Kama hawawasikii Musa na manabii, hawatashawishwa hata kama mmoja atafufuka kutoka kwa wafu. Luka 16:31 .

**7. Andiko la Waebrania 10:26, 27 laonekana kuonyesha kwamba mtu akitenda dhambi moja tu kimakusudi baada ya kujua vizuri kabisa, basi, yeye amepotea. Je, hii ni sahihi?**

Hapana! Mtu yeyote anaweza kuungama dhambi kama hiyo na kusamehewa. Biblia haisemi hapa juu ya tendo au dhambi moja bali juu ya kuendelea kwa kiburi katika dhambi na kukataa kujisalimisha kwa Kristo baada ya mtu kujua vyema zaidi. Tendo kama hilo humhuzunisha Roho Mtakatifu ( Waefeso 4:30 ) na hufanya moyo wa mtu kuwa mgumu hadi mtu anakuwa "amepita kuhisi au hawezi kuwa na hisia tena" (Waefeso 4:19 ) na kupotea. Biblia inasema, "Unizuie mtumishi wako na dhambi za kiburi, zisiwe na mamlaka juu yangu; Zaburi 19:13 .

**8. Je, si lazima mtu aelimishwe ili kuelewa Biblia?**

Hapana! Hata watu sahili wanaweza kuelewa ikiwa wamejisalimisha kwa Bwana ( Zaburi 19:7 ; 119:130 ; Mathayo 11:25 ).

**MASWALI YA CHEMSHA BONGO AU KWIZZ**

**1. Watu wataokolewa ambao (1)**
_____ wanafukuza pepo kwa Jina la Kristo.
_____ Daima Humpenda Kristo.
_____ Humkubali na mtii Bwana.

**2. Ni mambo gani matatu yaliyoorodheshwa hapa chini ambayo yatanihakikishia kupokea Ukweli kamili? (3)**
_____ Nimuulize daktari wangu wa magonjwa ya akili.
_____ Niombee nuru.
_____ Nifanye kile ambacho mchungaji wangu anasema.
_____ Nitoe sadaka ya  ukarimu kanisani.
_____ Nijiadhibu vikali.
_____ Nipate elimu bora.
_____ Nimwombe Mungu ishara.
_____ Nijifunze Biblia.
_____ Nifuate ule Ukweli ambao sasa ninauelewa.

**3. Mungu ananiwajibisha kwa (1)**
_____ Kufanya kile ambacho shemashi wangu anapendekeza.
_____ Kufuata nyayo za wazazi wangu.
_____ Nuru niliyo nayo na ninayoweza kuwa nayo.

**4. Ninapogundua Ukweli mpya, ni lazima (1)**
_____ niupuuze.
_____ Nisubiri hadi nihisi nimevutiwa kuikubali.
_____ Nikubali na kuitii mara moja.

**5. Utii kamili kwa amri za Bwana ni (1)**
_____ Ni jambo ambalo haliwezekani kwa hali yoyote.
_____ Uhafarisayo na ni ushetani.
_____ Inawezekana kupitia Kristo pekee.

**6. Kutotii kwa makusudi (1)**
_____ Huongoza kwenye giza na uharibifu wa milele.
_____ Ni sawa kwa watenda kazi wa kanisa wenye bidii.
_____ Hupuuzwa na Mungu nikiwa mkaidi na nikimbisha Yeye.

**7. Upendo wa Kweli kwa Bwana (1)**
_____ Ni bora kuliko utii.
_____ Hufanya utiifu usiwe wa lazima.
_____ Hunifanya nimtii kwa furaha.

**8. Uhuru wa Kweli wa Kikristo unamaanisha (1)**
_____ Haki ya kufanya nipendavyo katika kila jambo.
_____ Haki ya kutomtii Mungu.
_____ Uhuru kutoka kwa uasi na utumwa wa shetani.

**9. Jambo la Ukweli linapokuwa wazi lakini sielewi kwa nini Mungu ananihitaji niitii, mimi ninapaswa (1)**
_____ Kusubiri hadi sababu iwe wazi.
_____ Kulikataa jambo hilo la Ukweli.
_____ Kulikubali na kulitii Neno la Mungu.

**10. Ni nani hasa anayewajibika kwa kutotii kote? (1)**
_____ Serikali.
_____ Wazazi wangu, ambao walinifundisha vibaya.
_____ Ibilisi.

**11. Kwa nini utii ni wa lazima? (1)**
_____ Kwa sababu Mungu ni mkuu kuliko mimi, na ninamwogoa sana.
_____ Kumzuia Mungu asikasirike.
_____ Kwa sababu ninampenda Mungu na ninataka kufuata sheria Zake ili niwe na tabia ya Kikristo.

**12. Kwa nini Mungu hawaangamizi wasiotii sasa hivi? (1)**
_____ Anaogopa.
_____ Anafurahia kutazama uovu ukiendelea.
_____ Anangoja hadi wote wawe na hakika kabisa juu ya upendo na haki Yake.

**Mpinga Kristo ni nani?**

**Maandiko: Danieli 7:7-8 , Danieli 7:24-25 , Ufunuo 13:18**

**Somo la 15**

Mpinga Kristo ni nani, au ni nini? Muungano mbaya, au mtu mwovu? Wengine wanasema kuonekana kwake bado ni katika siku zijazo. Wengine wanasema alionekana zamani sana katika siku za Roma ya kale. Lakini Biblia inaonyesha kwamba Mpinga yuko hai leo! Unabii wa Biblia unafundisha kwamba mamlaka hiyo ya mpinga-Kristo itakuwa na fungu muhimu katika matukio ya mwisho ya historia ya dunia. Je, Unajua yeye ni nani? Je, Una uhakika? Je, mimi naweza kuwa mpinga Kristo? Kivipi basi? Je, Unahitaji kuwa na hakika, kwa maana huwezi kuelewa matukio ya siku za mwisho hadi uelewe nguvu hii mbaya. Uwe tayari kwa mojawapo ya Miongozo ya Masomo inayovutia zaidi bado!

Mwongozo huu wa Masomo, unaotegemea Danieli sura ya 7, unamtambulisha waziwazi na bila kosa Mpinga Kristo. Lakini ni utangulizi tu. Masomo yajayo yatafunua maelezo ya baadhi ya shughuli zake ambazo zitakuwa na athari duniani kote. Mambo unayogundua leo yanaweza kukuchukiza au kukuhuzunisha, lakini tafadhali kumbuka kwamba unabii wa Danieli sura ya 7 unatoka kwa Yesu, ambaye anakupenda wewe na mimi. Omba mwongozo wa Mungu unapoingia katika somo hili la dharura. Hakikisha umesoma Danieli 7 kabla ya kusoma mwongozo huu.

Katika unabii, Mungu anatumia wanyama kufananisha mataifa.

**1. Sura inapoanza, Danieli anaona wanyama wanne wakipanda kutoka baharini. Katika unabii, mnyama anawakilisha nini? Bahari inawakilisha nini?**
"Huyo mnyama wa nne atakuwa ufalme wa nne juu ya dunia." Danieli 7:23 . "Maji ... ni watu, na makutano, na mataifa, na lugha." Ufunuo 17:15 .

**Jibu:** Wanyama wanawakilisha falme au mataifa. Maji huwakilisha umati wa watu au idadi kubwa ya watu.

Mnyama simba wa Danieli 7 anawakilisha ufalme wa Babeli.

**2. Wanyama wanne wa Danieli 7 wanawakilisha falme nne za ulimwengu (mstari 17, 18). Babeli, ufalme wa kwanza (Danieli 2:38, 39), inawakilishwa kama simba kwenye Danieli 7:4. (Angalia pia Yeremia 4:7 50:17, 43, 44 kwa Babiloni/Babeli anayefananishwa na simba mahali pengine.) "Mabawa ya tai" yanamaanisha nini? Je, "pepo nne" za mstari wa 2 zinawakilisha nini?**
"Bwana ataleta taifa juu yako ... kama tai arukavyo." Kumbukumbu la Torati 28:49 .

"Bwana wa majeshi asema hivi, ... kimbunga kikubwa kitainuka kutoka katika mipaka ya dunia. Na hao waliouawa na Bwana watakuwa siku hiyo, toka upande mmoja wa dunia hata upande wa pili wa dunia. ." Yeremia 25:32 , 33 .

**Jibu:** Mabawa ya tai yanawakilisha kasi.
(Angalia pia Yeremia 4:13 ; Habakuki 1:6-9 .) Upepo huwakilisha ugomvi, ghasia, na uharibifu. (Ona pia Ufunuo 7:1-3 .)

Dubu mwenye mbavu tatu mdomoni anafananisha Umedi na Uajemi.

**3. Dubu anawakilisha ufalme gani (Danieli 7:5)? Je! mbavu tatu katika kinywa chake zinafananisha nini?**

**Jibu:** Soma Danieli 8. Ona kwamba wanyama katika sura ya 8 wanafanana na wale walio katika sura ya 7. Danieli 8:20 inataja haswa Umedi na Uajemi kama ufalme unaotangulia mbuzi mkali, au Ugiriki, wa mstari wa 21. Ni ufalme wa pili wa ulimwengu., mamlaka sawa na dubu wa Danieli 7. Milki hiyo ilifanyizwa na makundi mawili ya watu.

Wamedi walikuja kwanza (wanaowakilishwa katika Danieli 7:5 na dubu aliyeinuka upande mmoja), lakini Waajemi hatimaye wakawa na nguvu zaidi (inayowakilishwa katika Danieli 8:3 na pembe ya pili ya kondoo dume iliyokua "juu zaidi," au ndefu zaidi). Zile mbavu tatu zinawakilisha serikali tatu kuu zilizotekwa na Umedi na Uajemi:

Lidia, Babeli, na Misri.

Chui mnyama wa Danieli 7 anawakilisha ufalme wa ulimwengu wa Ugiriki.

**4. Ugiriki, ufalme wa tatu (Danieli 8:21), unawakilishwa na chui mwenye mabawa manne na vichwa vinne (Danieli 7:6). Vichwa vinawakilisha nini? Mabawa manne yanawakilisha nini?**

**Jibu:** Vichwa hivyo vinne vinawakilisha falme nne ambazo milki ya Aleksanda Mkuu iligawanywa alipokufa. Majenerali wanne walioongoza maeneo hayo walikuwa: Cassander, Lysimachus, Ptolemy, na Seleuko. Mabawa manne (badala ya mawili kama simba) yanawakilisha kasi ya ajabu, ambayo ilikuwa kweli kwa ushindi wa Aleksanda (Yeremia 4:11-13 ).

Milki ya ulimwengu ya Rumi inafananishwa na mnyama mkubwa wa Danieli sura ya 7.

**5. Ufalme wa Kirumi, ufalme wa nne wa ulimwenguni, unawakilishwa na mnyama mbaya sana mwenye meno ya chuma na pembe 10 (Danieli 7:7). Pembe zinawakilisha nini?**

**Jibu:** Pembe 10 zinawakilisha wafalme 10 au falme ambazo Roma ya kipagani hatimaye iligawanyika ( Danieli 7:24 ). (Falme hizi 10 ni sawa na vidole 10 vya miguu ya sanamu inayofafanuliwa katika Danieli 2:41-44 .) Makabila ya washenzi waliokuwa wakimangamanga yalifagia milki ya Roma na kuwajitwalia vishemu vya ardhi vizuri kwa watu wao.

Makabila saba kati ya hayo 10 yalisitawi na kuwa nchi za Ulaya Magharibi za sasa, huku matatu yaking'olewa na kuharibiwa. Sehemu inayofuata itazungumzia falme hizo ambazo ziling'olewa.

1. Visigoths - Uhispania
2. Anglo-Saxons - Uingereza
3. Franks - Ufaransa
4. Alemani - Ujerumani
5. Burgundians - Uswisi
6. Lombards - Italia
7. Suevi - Ureno
8. Heruli - Walingolewa
9. Ostrogoths -Walingolewa
10. Vandals- Walingolewa

Pembe ndogo ya Danieli 7:8 inawakilisha Mpinga Kristo.

**6. Katika unabii wa Danieli 7, ni nini kinachofuata?**
"Nikaziangalia sana pembe hizo, na tazama, pembe nyingine ikazukia kati yao, ndogo, ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza ziling'olewa na mizizi yake; na tazama, katika pembe hiyo palikuwa na macho kama macho ya mwanadamu; kinywa cha kunena mambo makuu." Danieli 7:8 .
**Jibu:** Nguvu ya "pembe ndogo" inaonekana kutokezea baadaye. Ni lazima tuitambue kwa uangalifu kwa sababu Mungu huchukua nafasi kubwa au wakati

mwingi zaidi kuielezea kuliko zile falme zingine nne zikiunganishwa pamoja. Kwa nini basi? Kwa sababu sifa za kibiblia zinaitambulisha hiyo falme au pembe kuwa ni Mpinga Kristo wa unabii na historia. Lazima kusiwe na makosa au mashaka katika kushugulikia kitambulisho hiki au utambulisho huu.

Biblia inasema Mpinga Kristo angewatesa watu wa Mungu.
**7. Je, kuna vipengele/point wazi za utambulisho huu?**
**Jibu:** Ndiyo, Mungu anatupa sifa tisa za Mpinga Kristo katika Danieli 7 ili tuwe na uhakika wa utambulisho wake. Na ingawa wengine wanaweza kupata ukweli huu kutoka kwa Neno la Mungu kuwa chungu, lazima tuwe wanyoofu vya kutosha ili kuzikubali kama mapenzi yake yaliyofunuliwa. Sasa hebu tugundue mambo tisa ya Yesu ni nini:

A. “Pembe ndogo” au ufalme “wakazuka kati yao “pembe 10 zilizokuwa falme za Ulaya Magharibi ( Danieli 7:8 ) Kwa hiyo ungekuwa ufalme mdogo mahali fulani. katika Ulaya Magharibi.

B. Ingekuwa na mtu mkuu ambaye angeweza kwenye ubongo wake angezungumza kwa ajili yake ( Danieli 7:8 )

C. Angeng’oa au kuondoa mizizi ya falme tatu ( Danieli 7:8 )

D. Ungekuwa “wa aina tofauti na zile falme 10 nyingine ( Danieli 7:24 )

E. Ungefanya vita na “kuchakaza” au kuwatesa watakatifu (Danieli 7:21 , 25 )

F. Ingetokeza katika milki ya kipagani ya Kirumi Ufalme wa ulimwengu wa nne ( Danieli 7:7, 8 )

G. Watu wa Mungu (watakatifu) ‘wangetiwa mkononi mwake’ kwa ajili ya “wakati na nyakati na mgawanyiko wa wakati” ( Danieli 7:25 )

H. Ingesema “maneno makuu dhidi ya” Mungu au kumkufuru Mungu (Danieli 7:25) Katika Ufunuo 13:5, Biblia inasema mamlaka hiyohiyo inazungumza “mambo makubwa na makufuru.”

I. ‘Ingefikiri kubadili majira na sheria. .” Danieli 7:25 .

Usisahau kwamba mambo haya yote ya utambulisho yanatoka moja kwa moja katika Biblia. Haya si maoni ya baadhi ya binadamu au uvumi tu. Wanahistoria wanaweza kukuambia harakaharaka ni nguvu gani inayoelezewa hapa. Pointi hizi zinaweza kutoshea falme au nguvu moja tu, upapa. Lakini ili kuwa na hakika kabisa, hebu tuchunguze kwa makini pointi zote tisa, moja baada ya nyingine. Lazima kusiwe na nafasi iliyoachwa ya shaka.

Upapa unaenda na sifa hizi zote kwa uwazi, yaani alama zote tisa za utambulisho.

**8. Je, upapa unafaa mambo haya?**

**Jibu:** Ndiyo, ina sifa ya kila pointi/nukta kikamilifu. Tazama vipengele A hadi H hapa chini.

A. "Ilikuja kati ya" falme 10 za Ulaya Magharibi.
Eneo la kijiografia la mamlaka ya upapa lilikuwa huko Rumi, Italia kitovu cha eneo la Ulaya Magharibi.

B. Ni mwanadamu ndiye ambaye anazungumziwa hapa.
Upapa unakutana na alama hii ya utambulisho kwa sababu una mtu mmoja mkuu (papa) ambaye anazungumza kwa niaba yake.

C. Ungeweza kung'oa falme tatu.
Wafalme au wakuu wa Ulaya Magharibi kwa sehemu kubwa walikuwa Wakatoliki na waliunga mkono upapa katika kukua na mamlaka yake. Falme tatu za Waarian, hata hivyo, hazikuunga mkono upapa, yaani Vandals, Heruli, na Ostrogoths. Kwa hiyo Wafalme hawa Wakatoliki waliamua kwamba lazima wawatiishe au kuwaangamiza. Hivi ndivyo Dakt. Mervyn Maxwell, mwanatheolojia na mwanahistoria, alivyoeleza matokeo katika Gombo la 1, ukurasa wa 129, wa kitabu chake God Cares: wewe endelea kuombea ili na Mungu atakufungulia zaidi, maana unabiii unaendelea kufunuliwa zaidi kwa wale wanaosoma ili wasaidie wengine.

"Mfalme wa kikatoliki Zeno (474-491) alipanga mapatano na Waostrogoth mwaka 487 ambayo yalisababisha kutokomezwa kwa ufalme wa Arian Heruls mwaka 493. Na mfalme Mkatoliki Justinian (527-565) aliwaangamiza Waarian Vandals mwaka 534 na kwa kiasi kikubwa ilivunja nguvu za Waostrogothi wa Arian mwaka wa 538. Hivyo pembe tatu za Danieli, Waheruli, Wavandali, na Waostrogothi ziling'olewa na mizizi yake pia.' "Si vigumu kutambua kwamba upapa unalingana na hatua hii.

D. Ingekuwa "tofauti" au tofauti na falme zingine.
Upapa unajaza sifa hizi kwa uwazi kwa maelezo haya, pia. Ulitokea kama nguvu ya kidini na ulikuwa tofauti kabisa na asili ya falme zingine 10 za kilimwengu.

E. Ingefanya vita na watakatifu na kuwatesa.
Kwamba kanisa lilitesa watakatifu au watu ni jambo linalojulikana sana hata kwenye historia. Upapa unakiri waziwazi kufanya hivyo na hata kuomba msamaha angalia ziara ya Papa John Paul kule Israeli mwaka 2008. Hakika kuna ushahidi mwingi wa kuunga mkono. Hata wanahistoria wahafidhina wanadai kuwa huenda kanisa liliwaangamiza au kuwaua angalau watu milioni 50 kwaajili ya mambo ya imani ya kidini. Tutanukuu hapa kutoka vyanzo viwili: 1. " Jambo ambalo kwamba Kanisa la Rumi limemwaga damu isiyo na hatia zaidi kuliko taasisi nyingine yoyote ambayo imewahi kuwepo miongoni mwa wanadamu, haitahojiwa na Mprotestanti yeyote ambaye ana ujuzi wa kutosha wa historia.

The History of the Inquisition of Spain, D. Ivan Antonio Llorente inatoa takwimu hizi kutoka kwa Mahakama ya Kihispania ya Inkwizisheni pekee:

Watu 31,912 walihukumiwa na kuangamia kwa moto huo.
Watu 241,450 walihukumiwa adhabu kali.

F. Ungetokea katika ufalme wa nne wa chuma - ufalme wa kipagani wa Rumi. Tunanukuu mamlaka mbili juu ya jambo hili:

1. “Kanisa kuu la Kikatoliki lilikuwa kidogo zaidi ya Dola ya Kirumi kubatizwa ... Mji mkuu wa Milki ya zamani ya Kirumi ukawa mji mkuu wa dola ya Kikristo. Ofisi ya Pontifex Maximus iliendelea. katika ile ya papa.” 2

2. “Mambo yoyote ya Kirumi ambayo washenzi na Waarian waliacha ... [ilikuja] chini ya ulinzi wa Askofu wa Roma, ambaye alikuwa mtu mkuu huko baada ya kutoweka kwa mfalme. Kanisa la Roma kwa njia hii lilijisukuma kwa siri mahali hapo na kuwa Mmilki wa Ulimwengu wa Kirumi, ambayo ni mwendelezo wake halisi.” 3

Kwa hiyo, kwa mara nyingine tena, jambo hilo linajaza sifa ya upapa.

G. Watu wa Mungu (watakatifu) “wangetiwa mkononi mwake” kwa “wakati na nyakati na mgawanyo wa wakati.” Danieli 7:25 .

Mambo kadhaa yanahitaji ufafanuzi kuhusiana na jambo hili:

1. Wakati ni mwaka, nyakati ni miaka miwili, na mgawanyo wa wakati ni nusu mwaka. The Amplified Bible inaitafsiri: “miaka mitatu na nusu.” 4

2. Kipindi hiki cha wakati kinatajwa mara saba ( Danieli 7:25 12:7 Ufunuo 11:2 , 3 12:6 , 14 13:5 ) katika vitabu vya Danieli na Ufunuo: mara tatu kwa wakati, nyakati, na nusu wakati mara mbili kama miezi 42 na mara mbili kama siku 1,260. Kulingana na kalenda ya siku 30 iliyotumiwa na Wayahudi, nyakati hizi zote ni kiasi sawa cha wakati:

miaka 3 1/2 = miezi 42 = siku 1,260.

3. Siku moja ya kinabii ni sawa na mwaka mmoja halisi (Ezekieli 4:6 Hesabu 14:34 ).

4. Hivyo, pembe ndogo (Mpinga Kristo) ilipaswa kuwa na nguvu juu ya watakatifu kwa siku 1,260 za kinabii au miaka 1,260 halisi.

5. Utawala wa upapa ulianza mwaka 538 BK, wakati wa mwisho kati ya falme tatu za Waariani zilizokuwa zikipingana zilipong’olewa. Utawala wake uliendelea hadi 1798 wakati jenerali wa Napoleon, Berthier, alipomchukua papa mateka akiwa na matumaini ya kumwangamiza Papa Pius VI na mamlaka ya kisiasa, ya kilimwengu ya upapa. Kipindi hiki cha wakati ni utimizo kamili wa unabii wa miaka 1,260. Pigo hilo lilikuwa jeraha la mauti kwa upapa, lakini jeraha hilo lilianza kupona na linaendelea kupona leo.

6. Kipindi hiki hiki cha mateso kinatajwa katika Mathayo 24:21 kama kipindi kibaya zaidi cha mateso ambayo watu wa Mungu watapata. Mstari wa 22 unatuambia kwamba ilikuwa yenye kuumiza sana hivi kwamba hakuna hata nafsi moja ambayo ingeokoka ikiwa Mungu hangeifupisha. Lakini Mungu alifupisha. Mnyanyaso huo uliisha muda mrefu kabla ya papa kuchukuliwa mateka mwaka wa 1798. Ni wazi kuona kwamba jambo hili, vilevile, linapatana na upapa.

H. Ingezungumza "maneno makuu" ya kufuru "dhidi ya Aliye Juu [Mungu]." Kukufuru kuna maana mbili katika Maandiko:

1. Kudai kusamehe dhambi ( Luka 5:21 ).

2. Kudai kuwa Mungu ( Yohana 10:33 ).

Je, hatua hii inafaa upapa? Ndiyo!

Hebu kwanza tuangalie ushahidi wake unaodai kusamehe dhambi: "Je! Kuhani kweli husamehe dhambi, au anatangaza tu kwamba zimeondolewa? Kristo."

5 Upapa unazidi kumpuuzia Yesu kwa kuanzisha utaratibu wa kuungama kwa kuhani wa kidunia, na hivyo kumtoa Yesu kama, Kuhani wetu Mkuu ( Waebrania 3:1 ) 8:1 , 2 ) na Mpatanishi pekee ( 1 Timotheo 2:5 ).

Kisha zingatia uthibitisho wake anaodai kuwa yeye ni Mungu: "Sisi [mapapa] tunashikilia juu ya ardhi hii mahali pa Mungu Mwenyezi."

6 Hapa kuna jingine: "Papa si mwakilishi wa Yesu Kristo tu, bali yeye ni Yesu Kristo, Mwenyewe, aliyefichwa chini ya pazia la mwili.

7 Ni dhahiri jambo hili, vile vile, linajaza sifa za upapa.

I. Angefikiri "kubadilisha nyakati na sheria."
Katika Mwongozo wa Masomo ujao tutashughulikia "nyakati" ya nukta hii ina maana gani. Ni mada kuu na inahitaji kuzingatiwa au kushugulikiwa tofauti. Lakini Je, ni vipi kuhusu kubadilisha "sheria"? The Amplified Bible inatafsiri "sheria kama neno la wingi" kama "sheria kama neno la umoja/singular." Rejelea ni kubadili sheria ya Mungu. Bila shaka, hakuna yeyote anayeweza kweli kuibadilisha ya Mungu (awe kiumbe au Mungu Mwenyewe), lakini je, upapa umejaribu kufanya hivyo? Jibu ni "ndiyo."

Katika katekisimu zake, upapa umeacha amri ya pili dhidi ya kuabudu sanamu na umefupisha amri ya nne kutoka maneno 94 hadi nane na kuigawanya amri ya kumi katika amri mbili (maneno yamehesabiwa Kingereza, fanya bidii nawe ukayahesabu Kiswahili). (Angalia hili mwenyewe. Linganisha Amri Kumi katika katekisimu yoyote ya Kikatoliki na orodha ya Mungu ya amri katika Kutoka 20:3-17.)

Hakuna shaka kwamba mamlaka ya pembe ndogo ya Danieli sura ya 7 (Mpinga Kristo) ni upapa. Hakuna taasisi/shirika lingine linaloweza lolote linaloweza kujaza pointi za sifa  hizi tisa. Na kwa bahati mbaya, haya sio mafundisho mapya. Kila Mwanamatengenezo bila ubaguzi, alizungumza juu ya upapa kama Mpinga Kristo. 8

**Maneno ya Kujali na Kuleta mfadhaiko**
Ili wengine wasifikiri kwamba tunawashambulia Wakristo wenzetu kwa kuitambua mamlaka hii yenye pembe ndogo, tafadhali kumbuka kwamba unabii huo unalenga mfumo fulani na si mtu binafsi. Kuna Wakristo waaminifu, ambao ni wacha Mungu katika makanisa yote, pamoja na imani ya Kikatoliki. Danieli sura ya 7 ni ujumbe wa hukumu na marekebisho juu ya taasisi kubwa ya kidini ambayo iliafikiana na upagani, kama vile makanisa mengine mengi yaliyotokea baada yake.

**Unabii Unafichua Makosa ya Imani Zote**
Unabii mwingine unaonyesha makosa ya imani ya Kiprotestanti na Kiyahudi. Mungu ana watu Wake  wakweli katika dini zote. Watu wake wa wakweli (bila kujali imani yao) daima watakubali kwa unyenyekevu kusahihishwa na Bwana na hawatafunga masikio na mioyo yao dhidi Yake kwa kujilinda au kujihami. Tunapaswa kushukuru sana kwamba Neno la Mungu linasema kwa unyoofu pasipo upendeleo juu ya kila somo.

1 WEH Lecky, Historia ya Kuinuka na Ushawishi wa Roho ya Urazini (rationalism) katika Ulaya, Juzuu 2, uk. 40.

22 Alexander Clarence Flick, The Rise of the Medieval Church, uk. 148, 149.

3 Adolf Harnack, Ukristo ni nini? (New York: Putnam, toleo la pili, lililorekebishwa, 1901), uk. 269, 270.

4 The Amplified Bible, Zondervan Publishing House, Grand Rapids, Michigan 1962.

5 Joseph Deharbe, SJ, Katekisimu Kamili ya Dini ya Kikatoliki (Mpya York: Schwartz, Kirwin & Fauss, 1924), p. 279.

6 Papa Leo XIII, Barua ya Ensiklika "The Reunion of Christendom" (tarehe 20 Juni 1894) trans. in the Great Encyclical Letters of Papa Leo XIII (New York: Benziger, 1903), p. 304.

7 Catholic National, Julai 1895.

8 R. Allen Anderson, Unfolding the Revelation, p. 137.
Malaika alimwambia Danieli kwamba unabii wa kitabu hiki ungetiwa muhuri hadi 1798, wakati wa mwisho.

**9. Je! Danieli hakuambiwa atie muhuri kitabu chake mpaka "wakati wa mwisho"? ( Danieli 12:4 ) Unabii wa Danieli utafunuliwa lini ili tuuelewe?**
**Jibu:** Katika Danieli 12:4 , nabii aliambiwa atie muhuri sehemu za kitabu hadi "wakati wa mwisho." Katika mstari wa 6 sauti ya malaika iliuliza, "Itakuwa hadi

lini hadi mwisho wa maajabu haya?" Mstari wa 7 unasema, "Itakuwa kwa wakati, nyakati na nusu." Malaika alimhakikishia Danieli kwamba sehemu ya kitabu inayohusu unabii wa nyakati za mwisho ingefunguliwa baada ya mwisho wa kipindi cha miaka 1260 cha udhibiti wa papa ambacho kilikuwa, kama tulivyojifunza hapo awali katika Mwongozo huu wa Somo, 1798.
Kwa hiyo wakati wa mwisho ulianza mwaka wa 1798. Bila shaka, kitabu cha Danieli kina ujumbe muhimu kutoka mbinguni kwa ajili yetu leo. Lazima kabisa tuelewe. Hakuna mahali pako wazi kama Mathayo 24:15, katika Yesu aliyosema kuhusu umuhimu wa kukisoma Kitabu hiki.
Mafundisho yote ya kidini lazima yalinganishwe na Maandiko ili kujua Ukweli na usahihi wake.

**10. Wakristo wengi leo wamepotoshwa sana kuhusu Mpinga Kristo. Kuamini uongo juu ya Mpinga Kristo kunaweza kusababisha mtu kudanganywa na kupotea kwa urahisi. Mtu anapaswa kufanya nini mafundisho mapya ya Biblia yanapopatikana?**
"Hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kama mambo hayo ndivyo yalivyo." Matendo 17:11 .

**Jibu:** Fundisho jipya la Biblia linapopatikana, njia pekee iliyo salama ni kulilinganisha kwa uangalifu na Maandiko ili kuona kama linapatana na Neno la Mungu.

11. Je, Niko tayari kufuata mahali Yesu anapoongoza, ingawa inaweza kuwa chungu?

**Maelezo ya Kumalizia**

Unabii mwingi muhimu kutoka katika vitabu vya Biblia vya Danieli na Ufunuo utaonyeshwa katika Miongozo ya Kujifunza ya Mambo ya Kweli Ajabu (Amazing Facts). Mungu ametoa unabii huu kwa:

A. Kufunua matukio ya mwisho ya dunia.

B. Kubainisha washiriki katika awamu ya mwisho ya vita kati ya Yesu na Shetani.

C. Kufichua wazi mipango miovu ya Shetani ya kututega na kutuangamiza sisi sote.

D. Kuonyesha usalama na upendo wa hukumu ambayo watakatifu wa Mungu watathibitishwa!

E. Mwinue Yesu, wokovu Wake, upendo, nguvu, rehema, na haki.

Wahusika Wakuu Watatokea mara kwa mara

Washiriki wakuu katika vita vya mwisho kati ya Yesu na Shetani watatokea mara kwa mara katika unabii huu. Watu hao wakiwemo: Shetani, Yesu, Marekani, upapa,

Uprotestanti, na (umizimu)kuwasiliana na pepo. Yesu anarudia na kupanua jumbe Zake kutoka kwa manabii ili kuhakikisha kwamba maonyo Yake ya upendo na ulinzi yanakuja kwa uwazi na uhakika.

**Jibu:**

**Maswali ya KUCHEUA AU Kufikiria**

**1. Siku zote nilifikiri Mpinga Kristo ni mtu badala ya shirika/taasisi. Je! nina makosa?**
Mpinga Kristo ni shirika ni taasisi--upapa. Maneno "macho ya mwanadamu" katika Danieli 7:8 , hata hivyo, yanaelekeza kwa kiongozi. Ufunuo 13:18 husema juu ya mwanadamu mwenye idadi fulani inayohusika. Katika Danieli sura ya 8, Ugiriki inawakilishwa na mbuzi na kiongozi wake, Aleksanda Mkuu, anafananishwa na pembe. Ndivyo ilivyo kwa Mpinga Kristo. Shirika ni upapa. Papa aliye madarakani ndiye mwakilishi wake. Unabii wa Danieli sura ya 7 hausemi kwamba mapapa ni waovu na kwamba Wakatoliki si Wakristo. Kuna Wakristo wengi Wakatoliki wachangamfu na wenye upendo. Mfumo huo, hata hivyo, unaitwa Mpinga Kristo kwa sababu umechukua mamlaka ya Yesu na kujaribu kubadilisha sheria Yake.

**2. Je, unafikiri ni busara kwa mtu au Mkristo kupitisha sheria za kulazimisha kila mtu awe Mkristo?**
Hapana, siyo busara. Biblia iko wazi kwamba wote wanapaswa kuwa na uhuru wa kuchagua mwelekeo wanaotaka kufuata katika mambo yanayohusu dhamiri ( Yoshua 24:15 )—hata kama wanaamua kumkana Mungu na kutoamini kwamba kuna Mungu. Mungu aliwaruhusu Adamu na Hawa wachague kutotii ingawa jambo hilo lilimuumiza Yeye Mungu, sisi na yeye Hawa Mwenyewe. Ibada ya kulazimishwa haikubaliki kwa Mungu. Ibada ya kulazimishwa ni njia ya shetani. Njia ya Mungu ni ushawishi wa upendo. Historia inaonyesha kwamba karibu kila wakati kanisa lilipopitisha sheria za kutekeleza imani yake, mateso na mauaji ya wengine yalitokeza. Hili ni somo tunaloweza kujifunza kutokana na historia ya Enzi ya Kati ya pembe ndogo.

**3. Labda sijaelewa, lakini dhana yangu daima imekuwa kwamba Mpinga Kristo angekuwa kiumbe mwovu ambaye alimpinga Mungu kwa waziwazi. Je, dhana hii si sahihi?**
Kwa kawaida tunachukulia neno "anti" kumaanisha "dhidi". Lakini katika "Mpinga Kristo" ina maana "mahali pa" au "badala ya". Mpinga Kristo ana hatia ya kuchukua mamlaka ya Mungu au kusema yeye ni badala ya Mungu. Inadai:

A. Makuhani wake wanasema wana uwezo wa kusamehe dhambi ambazo ni Mungu pekee Ndiye awezaye kufanya hivyo (Luka 5:21 ). Mfumo wa ukuhani haupo tena ulimwenguni baada ya Yesu kufa kwaajili ya wenye dhambi, Yeye Ndiye kuhani peke yake, kuna wachungaji, makasisi, maaskofu, mapadri nk, ila hakuna kuhani tena duniani. Hakuna binadamu ambaye ni kuhani tena.

B. Kubadilisha sheria ya Mungu kwa kuacha amri ya pili (ya kuabudu sanamu) na kugawanya ya kumi katika sehemu mbili. Sheria ya Mungu haiwezi kubadilishwa ( Mathayo 5:18 ).

C. Kwamba papa ni Mungu duniani.

Mpango **Asili wa Shetani (original plan)**

Mkakati wa asili wa Shetani (mbinguni) ulikuwa kushika nafasi na mamlaka ya Mungu. Kusudi lake lilikuwa kumfukuza Mungu na kutawala mahali pake. (Angalia Mwongozo wa 2 wa Somo.) Shetani alipofukuzwa kutoka mbinguni, lengo lake halikubadilika, bali lilizidi kuongezeka jazba. Kwa karne nyingi amejitahidi (akitumia mashirika mbalimbali ya kibinadamu) kumdharau Mungu na kuchukua nafasi Yake.

**Mpinga Kristo Aonekana Kuwa mtu wa Kiroho**

Shetani analenga kuchukua mahali pa Mungu katika siku hizi za mwisho kwa kuwadanganya watu wamfuate Mpinga Kristo, ni mtu anayeonekana kuwa wa kiroho na mtakatifu ila anatimiza ajenda za adui. Kusudi kuu la unabii wa Danieli na Ufunuo ni kufichua mitego na mikakati ya Shetani na kuwaongoza watu kutia nanga ndani ya Yesu na Neno Lake kwa usalama (Merikebu yao ya imani isivunjike).

**Mpinga Kristo Atawadanganya Wengi**

Watu wengi watamfuata Mpinga Kristo ( Ufunuo 13:3 ), wakifikiri kwamba wanamfuata Kristo. Wateule pekee ndio watakuwa salama ( Mathayo 24:23 , 24 ). Watakuwa salama kwa sababu wanalijaribu/wanapima kila mafundisho ya kiroho na kiongozi kwa Maandiko ( Isaya 8:20 ). Udanganyifu wa kidini uko kila mahali leo. Sisi hatuwezi kuwa makini sana kwani hali ni tete!

**4.Je,Bibliahaisemikatika1Yohana2:18-22kwambakunawapingaKristowengi?**

Ndiyo, kumekuwa na wapinga Kristo wengi katika historia ambao wamefanya kazi dhidi ya ufalme wa Mungu. Hata hivyo, kuna chombo kimoja tu ambacho kinatimiza hasa sifa zote zilizotabiriwa za Mpinga Kristo. Katika Danieli sura ya 7 na 8 na Ufunuo sura ya 13 , utapata angalau sifa 10 zinazomtambulisha Mpinga Kristo. Alama hizi 10 za utambuzi zinaweza kutimizwa katika chombo kimoja tu, yaani upapa.

**5. Katika unabii, je ishara ya "mnyama" ina maana ya tabia za "kinyama"?**

Hapana kabisa. Mungu hutumia ishara ya mnyama kuashiria mtawala, taifa, serikali, au ufalme. Ni njia Yake ya kuonyesha serikali katika unabii.Hata sisi tunafanya kwa kiwango fulani: Tumeonyesha Urusi kama dubu, Marekani kama tai, Kenya, Rwanda, Burundi na Congo ni Simba, Rwanda ina nyani pia, Uganda kama Korongo, Malawi kama Swala, Tanzania kama Twiga, Mayote kama Simba wa baharini, na Oman ina Swala aitwaye Orxy n.k. Alama ya "mnyama" si neno la kudhalilisha, lisilo na heshima. Ni sawa na "mnyama" au "kiumbe". Hata Kristo anaonyeshwa kama Mwana-Kondoo na Yohana Mbatizaji ( Yohana 1:29 ) na mtume Yohana ( Ufunuo 5:6 , 9 , 12 , 13 ). Neno "mnyama" linatumiwa na Mungu kutupa ujumbe kuhusu mataifa na viongozi, wema na uovu.

**Maswali au Kwizz au chemsha bongo**

**1. Ni falme gani nne za ulimwengu zinazowakilishwa na mifano ya hayawani katika Danieli sura ya 7 ? (4)**

_____ Uswidi.
_____ Misri.
_____ Ugiriki.
_____ Uchina.
_____ Umedi-Uajemi.
_____ Japan.
_____ Babeli.
_____ Iraki.
_____ Rumi.

**2. Katika unabii wa Biblia, mnyama anawakilisha (1)**

_____ Kompyuta.
_____ Ufalme au taifa.
_____ Kiumbe au mgeni.

**3. Pembe 10 juu ya mnyama mkubwa huwakilisha (1)**

_____ Miaka kumi.
_____ Miji kumi maalum.
_____ Malaika.
_____ Utajiri.
_____ Falme ambazo Rumi ya kipagani hatimaye iligawanyika.

**4. Ni makabila au mataifa mangapi "yaliyong'olewa" na mamlaka ya pembe ndogo? (1)**

_____ Nane.
_____ Moja.
_____ Sita.
_____ Tatu.

**5. Mamlaka ya pembe ndogo, au Mpinga Kristo, inawakilisha (1)**

_____ Mmoja wa majemadari wa Babeli.
_____ Mtawala mwovu kutoka siku za Roma ya kipagani ya kale.
_____ Nguvu mbaya itakayotokea baada ya ujio wa pili wa Yesu.
_____ Kutomwamini Mungu.
_____ Upapa.

**6. Angalia taarifa za Kweli kuhusu nguvu ya pembe ndogo (Mpinga Kristo) kutoka kwenye orodha iliyo hapa chini: (3)**

_____ Ilitoka Misri.
_____ Ingewatesa watu wa Mungu.
_____ Iliibuka mara baada ya Babeli kuanguka.
_____ Hunena maneno makuu dhidi ya Mungu.
_____ Ilijaribu kubadilisha sheria ya Mungu.

**7. Katika unabii, "wakati, nyakati, na nusu wakati" ni mfano wa (1)**
_____ Siku tatu na nusu halisi.
_____ miaka 42.
_____ miaka 1,260 halisi.

**8. "Wakati wa mwisho" ulianza lini? (1)**
_____ BK 31
_____ BK 1991
_____ BK 588
_____ BK 1798

**9. Mpinga Kristo ni shirika/taasisi, badala ya mtu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**10. Mpinga Kristo yupo leo. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**11. Mungu anataka kuwalazimisha watu wafanye ibada ya Kweli kwa sheria. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**12. Kukamatwa kwa Jenerali Berthier kwa papa kuliuumiza tu upapa. Jeraha lake la kuua lilianza kupona na linaendelea kupona leo. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**13. Ni kipengele gani kutoka kwenye orodha iliyo hapa chini ni muhimu kwa usalama wa kiroho kwa watu wa Mungu katika siku hizi za mwisho? (1)**
_____ Jifunze kuhubiri.
_____ Omba sana hadharani.
_____ Pima kila mafundisho ya kidini kwa Biblia.

## Ujumbe wa Malaika Wanaoruka Angani

### Somo la 16

Malaika ni viumbe halisi, yaani wapo! Wakati fulani huitwa makerubi au maserafi, roho hizi zenye nguvu zinazohudumu huonekana katika historia yote ya Biblia. Mara nyingi wanaonekana wakiwalinda na kuwaongoza watu wa Mungu, na wakati mwingine kuadhibu maovu - lakini moja ya misheni yao muhimu zaidi ni kufunua na kufafanua unabii. Je, unajua Mungu amesema jambo la pekee kupitia malaika Zake kwa watu waliofadhaika sana katika ulimwengu wetu wenye shughuli nyingi? Katika Ufunuo 14, Mungu anafunua baadhi ya jumbe za kutisha za siku za

mwisho zilizowekwa katika mfano wa malaika watatu wanaoruka. Jumbe hizi ni za maana sana, hivi kwamba zinapokamilika, Yesu anarudi! Mwongozo huu utakupa muhtasari wa kufungua macho, na miongozo minane ifuatayo itawasilisha maelezo ya ajabu. Shikilia kiti chako usije kuanguka kwa jumbe hii nzito... Ujumbe binafsi wa Mungu kwako uko karibu kuelezwa!

Kitabu cha Ufunuo kinamfunua Yesu kwa namna ya pekee. Huwezi kuzungumzia Injili ya Milele bila ya kuzungumzia mambo ya malaika hawa watatu. Je, tutazamie kuona malaika watatu siku moja angani?

1. MALAIKA WA KWANZA ANAONYESHA IBADA PEKEE ambayo ni ya KWELI , MAANA YAKE MCHE MUNGU NA KUMTUKUZA, KWANINI KWASABABU SAA YAKE YA HUKUMU IMEKUJA NA HIVYO USIWAACHE WATU WABWETEKE NA KUTOJITAYARISHA, KWANINI TUMCHE MUNGU KWA VILE YEYE NDIYE MUUMBAJI MKOMBOZI NA MDUMISHAJI, HIVYO CHUNGA SANA KUNA SHERIA YA KUMWABUDU, YAANI kuna IBADA MOJA TU ambayo ni YA KWELI , NA YEYE ANAIELEZA HAPA

2. MALAIKA WA PILI ANATOA ONYO KWA YULE ATAKAYEAMUA KUJIFANYIA IBADA ILE ANAYOTAKA yeye WAKATI WA HUKUMU ITAKUWAJE BASI, ANATUPA ONYO KILE KITAKACHOTOKEA KATIKA KUFANYA IBADA YA UONGO NASI TUNAPASWA KUWAAMBIA WATU ILI WAJUE na hivyo WASIJE WAKAANGAMIA

3. MALAIKA WA TATU ANAELEZA ADHABU YA IBADA YA UONGO, KWAMBA WATU WATAKUNYWA GHADHABU YA MVINYO WA MUNGU ISIYOCHANGANYWA, JE UNAWEZA KULETA HABARI NJEMA BILA KUSEMA IBADA YA KWELI, LA! Huwezi, JE UNAWEZA KULETA HABARI NJEMA BILA MATOKEO YA KUWA NA IBADA NYINGINE ambayo ni tofauti na ya Mungu? KUMBE UJUMBE HUU wa malaika watatu, UNAHUSU IBADA! KAMA NI YA KWELI INABIDI IWE HIVI, KAMA NI YA UONGO huwa inakuwa vile. HUKUMU IMEANZA TOKA SASA TUWAAMBIE WATU, HATUWEZI KUWA MBWA ASIYEBWEKA, ndiyo SISI SI POLISI WA WATU ILA TUSIPOWAAMBIA WATU KUTAKUWA NA NIN BASI? Soma zaidi uelewe vizuri. Ibada si jambo linalokupendeza mwenyewe au la uamuzi wako mwenyewe, bali ni la Uamuzi wa Mungu!

**1. Kwa nini tunajifunza Ufunuo? Je, si Kitabu hiki kimefungwa?**

**Jibu:** Kuna sababu sita muhimu za kusoma Ufunuo:

A. Haujawahi kutiwa muhuri ( Ufunuo 22:10 ). Mabishano ya muda mrefu kati ya Kristo na Shetani, pamoja na mikakati ya shetani na mipango ya hila ya siku za mwisho, yanafichuliwa katika Ufunuo. Shetani hawezi kuwanasa kwa urahisi watu wanaojua mapema udanganyifu wake au hila za uongo, kwa hiyo anatumaini kwamba watu wataamini kwamba kitabu Ufunuo kimetiwa muhuri.

B. Jina lenyewe "Ufunuo" linamaanisha "kufunua," "kufungua," au "kuweka wazo" kinyume kabisa cha kutiwa muhuri. Daima imekuwa wazi.

C. Ufunuo ni kitabu cha Yesu kwa namna ya pekee. Kinaanza kwa kusema "Ufunuo wa Yesu Kristo." Hata inatoa picha ya neno juu Yake katika Ufunuo 1:13-16 . Hakuna kitabu kingine cha Biblia kinachomfunua Yesu na maagizo na mipango Yake ya siku za mwisho kwa kazi Yake na watu Wake kama vile Ufunuo.

D. Ufunuo kimsingi kimeandikwa kwa ajili ya watu wa siku zetu, watu wa kabla tu ya kurudi kwa Yesu ( Ufunuo 1:1-3 ) 3:11 22:6 , 7 , 12 , 20 ).

E. Baraka ya pekee inatamkwa juu ya wale wanaosoma Ufunuo na kutii ushauri Wake ( Ufunuo 1:3 ) 22:7 ).

F. Ufunuo unaeleza watu wa Mungu wa nyakati za mwisho na kanisa kwa uwazi wa kushangaza. Huifanya Biblia kuwa hai unapoona matukio ya siku za mwisho yanayoonyeshwa katika Ufunuo yakitukia. Pia inaeleza kwa usahihi kile ambacho kanisa la Mungu lazima liwe linahubiri katika siku za mwisho (Ufunuo 14:6-14). Mwongozo huu wa Kujifunza utatoa muhtasari wa mahubiri hayo ili uweze kuyatambua unapoyasikia.

**Kumbuka:** Kabla ya kuendelea zaidi, tafadhali fungua Biblia yako na usome Ufunuo 14:6-14 .
Mungu hutumia malaika kuashiria ujumbe Wake wa mwisho wenye vipengele vitatu.

**2. Mungu aliagiza kanisa Lake kupeleka injili kwa kila kiumbe (Marko 16:15). Je, anaashiriaje kazi hii takatifu katika Ufunuo?**
"Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele aihubiri. ... Akafuatana na malaika mwingine, akisema ... . Malaika wa tatu akawafuata, akisema ....." Ufunuo 14 ; 6-9 .

**Jibu:** Neno "malaika" kihalisi linamaanisha "mjumbe," kwa hivyo inafaa kwamba Mungu atumie malaika watatu kuashiria kuhubiriwa kwa ujumbe Wake wa injili wenye alama tatu kwa siku za mwisho. Mungu anatumia ishara ya malaika kutukumbusha kwamba nguvu zisizo za kawaida zitaandamana na ujumbe.
Ujumbe wa Mungu wa tumaini la wakati wa mwisho lazima uwasilishwe kwa kila mtu duniani.

**3. Andiko la Ufunuo 14:6 linafunua mambo gani mawili muhimu kuhusu ujumbe wa Mungu wa siku za mwisho?**
"Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa." Ufunuo 14:6 .

**Jibu:** Mambo mawili muhimu ni: (1) kwamba ni "injili ya milele," na (2) kwamba ni lazima ihubiriwe kwa kila mtu duniani. Jumbe za malaika watatu zinakazia injili, ambayo inafanya iwe wazi kwamba watu wanaokolewa kwa imani katika

kumkubali-na Yesu Kristo pekee ( Matendo 4:12) Marko 10:26 , 27 ). Kwa kuwa hakuna njia nyingine ya wokovu iliyopo, ni uovu kudai kwamba kuna njia nyingine.

**Bidhaa Bandia za Shetani**
Marobota ya Shetani huku ni mengi nayo yanajumuisha mambo mawili: (1) wokovu kwa matendo, na (2) wokovu katika dhambi. Mambo haya mawili ya bandia yanafichuliwa na kuonyeshwa wazizwazi katika jumbe za malaika watatu. Wengi, bila kutambua, wamekubali moja ya makosa haya mawili na wanajaribu kujenga wokovu wao juu yake - jambo lisilowezekana kabisa. Pia lazima tusisitize kwamba hakuna mtu anayehubiri injili ya Yesu kwa wakati wa mwisho ambaye hajumuishi ujumbe wa malaika watatu.
Wale wanaomcha Mungu watapata furaha safi katika kumtumikia.

**4. Ujumbe wa malaika wa kwanza unahusu mambo gani manne tofauti?**
"Akisema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja; Ufunuo 14:7.

**Jibu:** A. Mche Mungu. Hii ina maana kwamba tunapaswa kuwa na kicho Kwake Mungu na kumwangalia kwa upendo, uaminifu, na heshima – tukiwa na shauku ya kufanya Maagizo Yake. Hii inatuepusha na uovu. "Kwa kumcha Bwana watu hujiepusha na uovu." Mithali 16:6 . Sulemani, mtu mwenye hekima, pia alisema, "Mche Mungu, nawe uzishike amri Zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu." Mhubiri 12:13 .

B. Mpe Mungu utukufu. Tunatimiza agizo hili tunapomtii, kumsifu, na kumshukuru Mungu kwa wema Wake kwetu. Moja ya dhambi kuu za siku za mwisho ni kutokuwa na shukrani ( 2 Timotheo 3:1 , 2 ).

C. Saa ya hukumu yake imefika. Hii inaashiria kwamba kila mtu anawajibika kwa Mungu, na ni tamko la wazi kwamba hukumu iko sasa. Tafsiri kadhaa zinasema "imekuja" badala ya "itakuja".

D. Mwabudu Muumba. Amri hii inakataa ibada ya sanamu ya kila aina - Ikiwemo na kujiabudu - na inakataa kabisa matengenezo, ambayo yanakana kwamba Mungu ni Muumba na Mkombozi. (Vitabu vingi na vipindi vya mazungumzo ya redio siku hizi vinasisitiza kujithamini yaani self esteem, jambo ambalo hupelekea mtu kujiabudu. Kujithamini kwa Mkristo ni katika Kristo, ambaye huwafanya watoto Wake kuwa wana na binti za Mfalme wa mbinguni.) Injili inajumuisha uumbaji na ukombozi wa ulimwengu na Bwana Mungu wa mbinguni. Kumwabudu Muumba ni pamoja na kumwabudu katika siku aliyoiweka kando kuwa ukumbusho wa Uumbaji (Sabato ya siku ya saba). Marejeo katika Ufunuo 14:7 yanahusu Sabato kwani yanawekwa wazi na Ukweli wa Maneno kwamba Mungu Ndiye "alifanya mbingu na nchi na bahari" , maelezo hayahaya yalitolewa moja kwa moja kutoka katika amri ya Nne ihusuyo Sabato ( Kutoka 20:11 ) na kutumika hapa.

Mizizi yetu ya kweli inapatikana kwa Mungu pekee, ambaye alituumba kwa mfano Wake hapo mwanzo. Wale ambao hawamwabudu Mungu kama Muumba,

hawataabudu chochote kingine, huenda wasigundue mizizi yao halisi. Ila Watu wa Mungu lazima watoke Babiloni.

**5. Malaika wa pili atoa maneno gani mazito kuhusu Babiloni? Malaika wa Ufunuo 18 anawaamuru watu wa Mungu wafanye nini?**
“Na malaika mwingine akafuata, akisema, Umeanguka Babeli.” Ufunuo 14:8 . “Nikaona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni. ... Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka Babeli ule mkuu.... Nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, .” Ufunuo 18:1-4 .

**Jibu:** Malaika wa pili anasema kwa dhati kwamba “Babiloni umeanguka,” na sauti kutoka mbinguni inawahimiza watu wote wa Mungu kutoka Babeli mara moja. Usipojua Babeli ni nini, unaweza kuishia humo ndani ya Babeli kirahisi sana. Fikiri juu ya jambo hili. Je, unaweza kuwa katika Babeli sasa?

Wale wanaoabudu mnyama na kupokea alama yake wataharibiwa na Mungu.
**6. Ujumbe wa malaika wa tatu unaonya kwa uzito juu ya nini?**
“Malaika wa tatu akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kupokea chapa yake katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, huyo atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu. “ Ufunuo 14:9 , 10 .

**Jibu:** Ujumbe wa malaika wa tatu unawaonya watu dhidi ya kumwabudu mnyama na sanamu yake na kupokea alama ya mnyama katika vipaji vya nyuso zao au mikono. Malaika wa kwanza anaamuru ibada ya Kweli. Malaika wa tatu anasimulia matokeo yenye kustaajabisha yanayohusiana na ibada ya uwongo. Je! unajua kwa hakika mnyama huyo ni nani? Na alama yake ni nini? Usipomjua vyema huyo mnyama ni nani na alama yake ni nini, unaweza kuishia kumwabudu bila kujua.
Watakatifu wa Bwana wa nyakati za mwisho watapata furaha yao kuu katika kumpendeza Yeye.

**7. Ni maelezo gani manne ambayo Mungu anatoa katika Ufunuo 14:12 ya watu Wake wanaokubali na kufuata jumbe za malaika watatu?**
“Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu.” Ufunuo 14:12 .

**Jibu:** A. Ni wavumilivu, wenye subira, na waaminifu hadi mwisho, agizo kubwa kwa kizazi hiki ni “fanya hivyo sasa”. Watu wa Mungu humfunua Yeyey kwa mwenendo wao wa subira na upendo.

B. Ni watakatifu, wametakaswa, kwa sababu wako upande wa Mungu kikamilifu.

C. Wanazishika amri za Mungu. Watu hawa wa Mungu wanatii kwa furaha Amri Zake Kumi na amri nyingine zote alizowapa. Kusudi lao la kwanza ni kumpendeza Yeye, ambaye wanampenda ( 1 Yohana 3:22 ).

D. Wana imani ya Yesu. Hii pia inaweza kutafsiriwa “imani katika Yesu.” Kwa

vyovyote vile, watu wa Mungu humfuata Yesu kikamilifu na kumwamini kikamilifu. Wakati wote wamesikia ujumbe wa Yesu wa wakati wa mwisho, Yeye atarudi duniani kuchukua watu Wake pamoja Naye mbinguni.

**8. Ni nini kinachotokea mara tu baada ya mafundisho ya ujumbe wa malaika watatu kwenda kwa watu wote?**
"Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya lile wingu ameketi mmoja kama Mwana wa Adamu, mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa Chake." Ufunuo 14:14.

**Jibu:** Mara tu baada ya mafundisho ya ujumbe wa malaika watatu kwa kila mtu, Yesu atarudi katika mawingu (Ujio Wake wa pili) kuchukua watu Wake hadi nyumbani kwao mbinguni. Wakati wa kutokea Kwake, kule kuzimwa kwa giza kwa miaka 1,000 kwa Ufunuo sura ya 20 kutaanza.

**9. Katika 2 Petro 1:12, mtume anazungumza juu ya "Kweli ya sasa." Anamaanisha nini?**

**Jibu:** Ukweli wa sasa ni kipengele cha injili ya milele ambacho kina dharura/uharaka maalum kwa muda fulani. Mifano ni:

***A. Ujumbe wa Nuhu wa Gharika*** (Mwanzo 6 na 7 2 Petro 2:5 ). Nuhu alikuwa mhubiri wa haki. Alifundisha upendo wa Mungu alipokuwa akionya ***kuhusu gharika inayokuja*** ambayo ingeharibu ulimwengu. **Ujumbe wa Gharika ulikuwa "Ukweli wa sasa wa wakati ule au Ukweli wa leo au Ukweli uliopo"** kwa wakati huo. Kilio chake cha haraka kilikuwa ***"ingia ndani ya safina."*** Na ujumbe huu ulikuwa muhimu sana kwamba ingekuwa ni kosa la kimaadili kutouhubiri.

***B. Ujumbe wa Yona kwa Ninawi*** ( Yona 3:4 ). ***"Ukweli wa sasa" wa Yona ulikuwa kwamba Ninawi ingeangamizwa katika muda wa siku 40.*** Yona pia alimwinua Mwokozi, na mji ukatubu. Hata hivyo, ***kupuuza onyo hilo la siku 40*** ingekuwa kukosa la uaminifu na jambo lisiloweza kusamehewa. Huo ulikuwa Ukweli wa sasa au wa wakati huo. Ujumbe huo ulifaa kwa wakati huo kwa njia ya pekee.

***C. Ujumbe wa Yohana Mbatizaji*** ( Mathayo 3:1-3 Luka 1:17 ). ***"Ukweli wa sasa" wa Yohana ulikuwa kwamba Yesu,*** Masihi, alikuwa karibu kutokea. Kazi yake ilikuwa kuwasilisha injili na kuwatayarisha watu kwa ***ujio wa kwanza wa Yesu.*** Kuacha kuhubiri kipengele hicho cha kuja kwa mara ya kwanza cha injili kwa siku yake lingekuwa jambo la kutisha ambalo hungependa hata kulifikiria.

**D. Ujumbe wa malaika watatu** ( Ufunuo 14:6-14 ). ***"Ukweli wa sasa" wa Mungu wa leo unapatikana katika*** jumbe za malaika watatu. Bila shaka, ***wokovu kupitia Yesu Kristo pekee ndio kiini cha jumbe hizi.*** Hata hivyo, ***"Ukweli uliopo"*** wa wale malaika watatu pia umetolewa ili ***kuwatayarisha watu kwa ajili ya ujio wa pili wa Yesu*** na ***kufungua macho yao kwa kuja kwa Shetani. yaani*** udanganyifu ***mkali*** na ***wenye kushawishi sana.*** Watu wasipoelewa jumbe hizi, Shetani atazikamata na kuziangamiza. Yesu alijua tulihitaji jumbe hizi tatu maalum, kwa hiyo kwa fadhili zenye upendo Yeye amezitoa. Hizi Hazipaswi

kuachwa. Tafadhali omba kwa bidii unapozichunguza hatua kwa hatua katika ***Miongozo minane ya Masomo kama ifuatavyo.***
Baadhi ya uvumbuzi wako unaweza kukushtua. Lakini yote yatakuwa ya kuridhisha moyo. Moyo wako utasisimka sana. Utahisi Yesu akizungumza nawe! Baada ya yote, hizi ni Jumbe Zake.

**10. Biblia inasema nani atakuja kutoa ujumbe wa "Kweli iliyopo" kabla ya siku kuu ya Bwana?**
"Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana iliyo kuu na kuogofya." Malaki 4:5 .

**Jibu:** Nabii Eliya. Kuna jambo la maana kuhusu Eliya na ujumbe wake, kama tutakavyoona katika maswali machache yanayofuata.
***Jumbe za Mungu za nyakati za mwisho*** pia huitwa ***ujumbe wa "Eliya".*** Wito kwaajili ya kufanya ***uamuzi.***

**11. Eliya alifanya nini ambacho kilimfanya Bwana kukita kwenye huduma yake?**
**Kumbuka:** Tafadhali fungua Biblia yako na usome kwa makini 1 Wafalme 18:17-40 kabla ya kujibu swali hili.

**Jibu:** Eliya aliwahimiza watu waamue ni nani wangemtumikia (mstari wa 21). Taifa karibu lote lilikuwa linaabudu sanamu. Watu walikuwa wamemwacha Mungu wa Kweli na amri Zake. Kulikuwa na nabii mmoja wa Mungu, Eliya, na manabii wa kipagani 450 wa Baali (mstari wa 22). Eliya alipendekeza kwamba yeye na waabudu-sanamu wajenge madhabahu na kuweka mbao na fahali juu yake. Kisha akapendekeza wamwombe Mungu wa Kweli ajifunue kwa kuwasha moto madhabahu Yake. Mungu wa kipagani hakujibu, lakini Mungu wa Kweli wa Eliya alituma moto kutoka mbinguni na kuteketeza dhabihu ya Eliya.

**Ujumbe Unadai Uamuzi**
Ujumbe wa Eliya ulikuja wakati wa shida kubwa ya kiroho na uasi wa kitaifa. Ulikuja na nguvu kutoka mbinguni hivi kwamba ulisimamisha uzembe wa kufikiria"shuguli za maisha zinaendelea kama kawaida" na kuvuta hisia za kitaifa. Kisha Eliya akasisitiza kwamba watu waamue ni nani wangemtumikia, Mungu au Baali. Kwa kusukumwa sana na kusadikishwa kabisa, watu walimchagua Mungu (mstari wa 39).
Yohana Mbatizaji aliwasilisha ujumbe wa "Eliya" wa siku zake. Wale wanaohubiri Ufunuo 14:6-14 wana ujumbe wa Eliya wa leo.

**12. Ujumbe wa Eliya una matumizi mawili. Unatumika kama ujumbe wa "Ukweli uliopo" ili kuwatayarisha watu kwa ujio wa kwanza wa Yesu na ujumbe wa "Ukweli wa sasa" ili kuwatayarisha watu kwa ujio wa pili wa Yesu. Yesu alisema nani alihubiri ujumbe wa Eliya ili kuwatayarisha watu kwa ajili ya ujio Wake wa kwanza?**
"Hajatokea aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji." "Na ikiwa mnataka kumpokea, huyo ndiye Eliya [Eliya], ambaye alikuwa aje." Mathayo 11:11 , 14 .

**Jibu:** Yesu aliita mahubiri ya Yohana ili kuwatayarisha watu kwa ajili ya ujio Wake wa kwanza "Eliya," au ujumbe wa Eliya. Ujumbe wa Yohana, kama katika siku za Eliya, ulionyesha Ukweli waziwazi kisha ukasisitiza uamuzi fulani. Biblia inasema juu ya Yohana Mbatizaji, "Yeye atakwenda ... katika roho na nguvu za Eliya [Eliya]." Luka 1:17 .

**13. Tunajuaje kwamba unabii huo una matumizi ya pili kwa wakati wetu kabla tu ya ujio wa pili?**
"Nitawapelekea Eliya nabii kabla haijaja siku ile iliyo kuu na kuogofya ya Bwana." Malaki 4:5 . "Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na itishayo." Yoeli 2:31.

**Jibu:** Tafadhali kumbuka kwamba ***matukio mawili*** yatatokea ***kabla ya kuja kwa "siku ya Bwana iliyo kuu na itishayo"*** inayotajwa katika Yoeli 2:31 . ***Moja,*** kuja ***kwa Eliya.*** Na ***mbili,*** Ishara ***kubwa mbinguni.*** Hii hutusaidia kupata matukio yote mawili. Siku ya giza ilitokea Mei 19, 1780. ***Usiku huohuo, mwezi ulionekana kama damu.*** Mathayo 24:29 inajumuisha ***ishara moja zaidi,*** kuanguka ***kwa nyota,*** ambayo ilifanyika Novemba 13, 1833. Kutokana na tukio hili, ***tunajua wakati wa mwisho u karibu. Ujumbe wa Eliya*** lazima uanze wakati fulani karibu au baada ya 1833, ***kabla ya kuja kwa siku kuu ya Bwana.***

**Ujumbe wa Eliya wa Pili Baada ya Ishara za Anga**
Ni dhahiri kwamba "ujumbe wa Eliya" wa Yohana hauhusu "ujumbe wa Eliya" wa pili kwa sababu ishara kuu za anga za Mungu zilionekana zaidi ya miaka 1,700 baada ya Yohana kuhubiri ujumbe wake. Ujumbe wa Eliya wa Yoeli 2:31 ulipaswa kuanza baada ya ishara hizo za anga mwaka 1833 na lazima tutayarishe watu kwa ajili ya ***ujio wa pili wa Yesu.*** Ujumbe ***wa "Kweli ya sasa" wa Ufunuo 14:6-14 unafaa kikamilifu. Ujumbe huu ulianza kuhubiriwa karibu 1844*** nauki***watayarisha watu ulimwenguni pote kwa ajili ya ujio wa pili wa Yesu*** (mstari wa 14), ambao utafanyika baada ya Jumbe zenye sehemu tatu kumfikia kila mtu duniani.

**Ujumbe Unadai Uamuzi**
Eliya alisisitiza maovu yakabiliwe moja kwa moja na kwamba wote waamue ni nani wangemtumikia. Ndivyo ilivyo na ujumbe wa Mungu wenye sehemu tatu kwa ajili yetu leo. ***Uamuzi lazima ufanywe. Ujumbe wa Mungu wenye sehemu tatu unamfichua Shetani na mipango yake. U***nafunua waziwazi ***upendo wa Mungu*** na ***matakwa Yake.*** Mungu anawaita watu leo warudi kwenye ibada ya Kweli, kumwabudu Mungu pekee. Kumtumikia na kuabudu kwa kujua mtu yeyote au kitu kingine chochote katika siku hii muhimu, ni sawa na kutokuwa mwaminifu na jambo hilo litasababisha kifo cha milele. Mungu alifikia mioyo kimuujiza katika siku za Eliya ( 1 Wafalme 18:37 , 39 ) na katika siku za Yohana Mbatizaji. Yeye Atafanya vivyo hivyo katika siku hizi za mwisho watu wanapoitikia ujumbe wa malaika watatu ( Ufunuo 18:1 ).

***Ujumbe wa mwisho wa Mungu wa Eliya utaleta familia pamoja katika shangwe, upendo, na furaha.***

**14. Ni baraka gani nyingine nzuri ambayo katika kuhubiriwa kwa Eliya (au ujumbe wa malaika watatu) itataletwa?**
"Eliya ... ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao." Malaki 4:5 , 6 .
**Jibu:** Mungu asifiwe! Ujumbe wa Eliya, au ujumbe wa malaika watatu, utawaleta wanafamilia pamoja katika uhusiano wa upendo, wa karibu, wa furaha na wa mbinguni. Ni ahadi yenye baraka jinsi gani basi!

***Jumbe za malaika watatu zinamlenga Yesu.***

**15. Neno "injili" linamaanisha "habari njema." Je, jumbe za malaika watatu za Ufunuo sura ya 14 hutoa habari njema?**

**Jibu:** Ndiyo kweli! Hebu tupitie habari njema tuliyopata katika muhtasari huu wa jumbe za malaika watatu:

a. Kila mtu atapata fursa ya kusikia na kuelewa injili ya siku za mwisho. Hakuna hata mmoja atakayerukwa.
b. Mipango mizuri na yenye nguvu ya shetani ya kuwanasa na kuwaangamiza watu itafichuliwa kwetu, kwa hiyo hatuhitaji kunaswa.
c. Nguvu zisizo za kawaida za mbinguni zitaandamana na Jumbe na kueneza ujumbe wa Mungu katika siku hizi za mwisho.
d. Watu wa Mungu watakuwa na subira. Yeye Anawaita "watakatifu."
e. Watu wa Mungu watakuwa na imani ya Yesu.
f. Watu wa Mungu, kwa upendo, watatii amri Zake.
g. Mungu anatupenda sana hata ametuma ujumbe wa pekee sana ili kututayarisha kwa ujio wa pili wa Yesu.
h. Ujumbe wa Mungu kwa siku hizi za mwisho utaleta wanafamilia pamoja katika upendo na umoja.
i. Msisitizo mkuu wa jumbe za malaika watatu ni kwamba wokovu umetolewa kwa kila mtu kupitia Yesu Kristo pekee. Yeye Anatoa haki Yake ili kufunika maisha yetu yaliyopita na anatupa haki Yake kwa miujiza kila siku ili tuweze kukua katika neema na kuwa kama Yeye kwelikweli au haswa. Pamoja Naye, hatuwezi kushindwa. Bila Yeye, hatuwezi kufanikiwa.

**Neno Ziada**

**Vidokezo vya jumbe za malaika watatu ambazo zitafafanuliwa katika Viongozo vijavyo ni:**

a. Saa ya hukumu ya Mungu imewadia!
b. Toka katika Babeli iliyoanguka.
c. Usiipokee chapa ya mnyama.

Habari njema nyingi zaidi zitafichuliwa unapojifunza kwa maombi masomo haya katika Miongozo minane ya Masomo yajayo. Utashangaa na kufurahishwa na mambo fulani, utashtushwa na kuhuzunishwa na mengine. Baadhi ya pointi zinaweza kuwa ngumu sana kuzikubali. Lakini kwa kuwa Yesu alituma ujumbe wa pekee kutoka mbinguni ili kusaidia na kuelekeza kila mmoja wetu kibinafsi katika siku hizi za mwisho, kwa hakika hakuna jambo la maana zaidi kuliko kuusikia, kuuelewa kikamilifu, na kuufuata ujumbe huu wa malaika watatu.

**16. Nimefarijika na kushukuru kwamba Yesu ana ujumbe wa pekee wa mambo matatu ili kuwaongoza na kuwasaidia watu Wake katika siku hizi za mwisho za dunia.**

**Jibu:**

**Maswali ya Kucheua na kKfikiria**

**1. Je, kila mtu duniani atafikiwa na ujumbe wa malaika watatu kabla ya kurudi kwa Yesu? Kwa kuwa mabilioni ya watu wanaishi sasa, Je hilo lawezekanaje?**
Ndiyo, itatokea kwa sababu Mungu aliahidi ( Marko 16:15 ). Paulo anasema injili ilienda "kwa kila kiumbe kilicho chini ya mbingu" katika siku zake ( Wakolosai 1:23 ). Yona, kwa neema ya Mungu, alifika mji mzima wa Ninawi chini ya siku 40 ( Yona 3:4-10 ). Biblia inasema Mungu atamaliza kazi YAKE na kuikata ( Warumi 9:28 ). Amini kwamba hilo litatokea. Litatokea haraka sana na katika siku zetu.

**2. Je, Musa na Eliya walionekana pamoja na Yesu wakati wa kugeuka sura (Mathayo 17:3) au ilikuwa nimaono tu?**

Tukio hilo lilikuwa halisi. Neno la Kiyunani "horama", lililotafsiriwa "maono" katika mstari wa 9, maana yake halisi ni "kile kilichoonekana". Musa alifufuliwa kutoka kwa wafu na kupelekwa mbinguni (Yuda 1:9 ), na Eliya baadaye alihamishwa kwenda mbinguni bila ya kukiona kifo ( 2 Wafalme 2:1 , 11 , 12 ). Watu hawa wawili, waliokuwa duniani na kuteseka sana kutokana na mashambulizi ya shetani na uasi wa watu wa Mungu, walielewa kile ambacho Yesu alikuwa akipitia. Walikuja kumtia moyo na kumkumbusha wale wote ambao wangehamishwa kwenda mbinguni katika ufalme Wake bila kuona kifo (kama Eliya) na kufufuliwa kutoka kaburini ili kuingia ufalme Wake (kama Musa) kwa sababu ya dhabihu Yake kwa ajili ya dhambi zetu.

**3. Kwa nini Yohana alisema yeye hakuwa Eliya (Yohana 1:19-21) Wakati Yesu alisema kwamba yeye ndiye (Mathayo 11:10-14)?**

Jibu linatokana na Luka 1:3-17 . Malaika aliyetangaza kuzaliwa kwa Yohana kuja alisema, "Elisabeti mkeo atakuzalia mtoto mwanamume, nawe utamwita jina lake Yohana. ... Huyo atakuwa mkuu mbele za Bwana. ... Naye atatangulia mbele zake. katika roho na nguvu za Eliya, kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na waasi wafuate hekima ya wenye haki, na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa." Mstari wa 13-17. Yesu alipomtaja Yohana kuwa Eliya, alikuwa akirejelea maisha yake, roho, nguvu, na kazi yake kuwa kama ile ya Eliya. Ndivyo

ilivyo kuhusu ujumbe wa Eliya wa siku hizi za mwisho. **Mkazo ni juu ya ujumbe, si mtu.** Kwa hiyo Yohana hakuwa Eliya ana kwa ana, bali alikuwa akiwasilisha ujumbe wa Eliya. ("Eliya" ni aina ya Kigiriki ya "Eliya".)

**4. Je, inawezekana kwa mtu kuwa anahubiri Ukweli kamili wa Yesu wa wakati wa mwisho kwa leo bila kujumuisha Jumbe za malaika watatu?**

Hapana! Ujumbe wa malaika watatu lazima ujumuishwe. Katika kitabu cha Ufunuo, Yesu Mwenyewe anafunua au kutaja ujumbe Wake wa wakati wa mwisho ( Ufunuo 1:1 ) na kusema waziwazi kwamba watu Wake wanapaswa kuendelea kufuata yale ambayo amefunua katika kitabu ( Ufunuo 1:3 ) 22:7 ). Kwa hiyo makasisi waaminifu wa nyakati za mwisho lazima wawe wanahubiri Jumbe za Yesu kutoka katika kitabu cha Ufunuo. Hili, bila shaka, linajumuisha kuhubiri ujumbe Wake maalum wa mambo matatu wa Ufunuo 14:6-14 .  Angalia kwamba Yesu anaziita Jumbe hizi "injili ya milele" katika mstari wa 6. Pia anasema lazima zipelekwe kwa kila mtu duniani kabla hajarudi kwa ajili ya watu Wake. Hapa kuna mawazo matatu mazito:

A. Hakuna anayehubiri "injili ya milele" ya Yesu isipokuwa ikiwa inajumuisha Jumbe za malaika watatu.

B. Hakuna mtu aliye na haki ya kuita jumbe zake injili ya milele ikiwa ataacha Jumbe za malaika watatu.

C. Ujumbe wa malaika watatu huwatayarisha watu kwa ajili ya ujio wa pili wa Yesu ( Ufunuo 14:12-14 ). Isipokuwa wewe  umezisikia, umezielewa, na kuzikubali Jumbe hizi tatu za Yesu za nyakati za mwisho, huenda usiwe tayari kwa ujio Wake wa pili.

**Jumbe Maalum kwa Wakati wa Mwisho**

Yesu, ambaye anajua tunachohitaji, alitupa jumbe tatu maalum kwa ajili ya wakati wa mwisho. Ni lazima tuzielewe na kuzifuata. Ibada ile ambayo Mungu ameandika tumpe, ndiyo tunapaswa kumpa, yeyote anayetaka kuleta ibada bandia aliyojitungia na isiyo katika Maandiko, basi kuna matokeo yake. Tunaambiwa tumche Mungu na kumtukuza, kwa maana saa Yake ya Hukumu imefika. Tunamwabudu kwasababu Yeye ni Muumba, Mkombozi na Mdumishaji. Anatoa onyo la ibada bandia, na adhabu ya ibada hiyo bandia isiyo kwenye Maandiko, au Kwenye Amri Zake. Hatuwezi kuhubiri Injili ya Milele bila ya kusisitiza kwamba Yeye Mungu Ndiye Muumbaji, Mkombozi na Mdumishaji. Na Kuna siku atakuja Kuihukumu dunia. Hatuwezi kuhubiri Injili bila kuwajulisha watu kwamba Hukumu inakuja, na Baada ya Hukumu hufuatia ijara/thawabu. Miongozo minane ifuatayo ya Masomo itafanya jumbe hizi kuwa wazi kwako.

**5. Luka 1:17 inasema ujumbe wa Eliya ulikuwa wa kuwageuza "wasiotii wapate hekima ya wenye haki". Hii ina maana gani?**

"Mwenye haki ataishi kwa imani." Warumi 1:17 . Wenye haki wana hekima ya kuweka wokovu wao juu ya imani katika Mwokozi. "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa

wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Matendo 4:12 . Ujumbe wa Yohana ulikuwa wa kufanya mambo kuwa wazi kwa wote. Imani ambayo imejikita kwa mtu yeyote au kitu chochote isipokuwa Yesu Kristo haiwezi kamwe kuwaokoa watu kutoka kwa dhambi na kusababisha maisha yaliyobadilika. Watu lazima wasikie na kuelewa jambo hili kuu la Ukweli. Ukweli huu pia ndio moyo hasa wa ujumbe wa Mungu wa Eliya wa mambo matatu kwa siku ya leo.

**Maswali ya Maswali**

**1. Malaika watatu wa Ufunuo 14 (1)**
_____ Ni halisi na wanapaswa kupiga kelele kwa sauti kubwa ili wasikilizwe.
_____ Wakilisha ujumbe wa Mungu wa siku za mwisho unaosonga kwa kasi na nguvu.
_____ Ni taswira ya mawazo ya mtu fulani.

**2. Ni mambo gani hapa chini yanaeleza Ukweli kuhusu Ufunuo? (3)**
_____ Kitabu kimefungwa.
_____ Jina linamaanisha "kufunua" au "kufichua."
_____ Inaeleza ni ujumbe gani ambao watu wa Mungu watahubiri katika siku za mwisho.
_____ Ina taswira ya maneno ya Yesu.
_____ Mungu alitangaza laana kwa wale wanaoisoma.

**3. Ujumbe wa wale malaika watatu lazima uende kwa kila mtu kabla Yesu hajarudi. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**4. Ujumbe wa malaika wa kwanza unasisitiza yafuatayo: (3)**
_____ Ni injili ya milele inayowasilishwa.
_____ Haiwezi kueleweka.
_____ Uibukaji ni nadharia nzuri ya Kikristo.
_____ Hukumu sasa iko kwenye kikao.
_____ Tunapaswa kumheshimu na kumwamini Mungu kikweli.
_____ Kila mtu anapaswa kuabudu chochote anachotaka.

**5. Ujumbe wa malaika wa pili unasema Babeli umeanguka, na malaika wa Ufunuo 18 anawahimiza watu wa Mungu walioko Babeli watoke nje. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**6. Ujumbe wa malaika wa tatu unawahimiza watu wote wa Mungu kupokea alama ya mnyama. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**7. Andiko la Ufunuo 14:12 linasemaje kuhusu watu wa Mungu? (2)**

_____ Wana subira.
_____ Wao ni watakatifu.
_____ Hawaamini katika Amri Kumi.
_____ Wana imani ndogo sana.

**8. Nini kinatokea mara baada ya injili kumfikia kila mtu? (1)**
_____ Mataifa yote yameongoka.
_____ Mungu anajenga upya New York na London.
_____ Kuja kwa Yesu mara ya pili kunatokea.

**9. Je, ni ujumbe upi kati ya zifuatazo ambao ni "Ukweli wa sasa" au Ukweli wa leo? (1)**
_____ Ujumbe wa Yona kwa Ninawi.
_____ Ujumbe wa Nuhu kabla ya Gharika.
_____ Ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo 14:6-14 .

**10. Ni mambo gani ambayo ni ya Kweli kuhusu jumbe za malaika watatu? (8)**
_____ Jumbe hizi zinahubiriwa sasa.
_____ Jumbe hizi zinasisitiza wokovu kupitia Yesu Kristo pekee.
_____ Zinaweza pia kuitwa "ujumbe wa Eliya."
_____ Eliya atatokea kibinafsi ili kusaidia kuziwawasilisha.
_____ Zinasisitiza maadili ya Kikristo ya Uibukaji.
_____ Watu wengi hawatawahi kuzisikia.
_____ Zitaleta wanafamilia pamoja katika uhusiano wa karibu, wa upendo.
_____ Nguvu zisizo za kawaida zitafuatana nao.
_____ Zinasaidia kuwatayarisha watu kwa ujio wa pili wa Yesu.
_____Malaika wale wanawakilisha Wajumbe, na wanatuwakilisha sisi tunaopeleka ujumbe wa Malaika watatu, na siyo kwamba tutaona Malaika wakiruka kuleta huu ujumbe, bali sisi ndiyo wajumbe ambao tutaupeleka huu hizi jumbe Tatu
_____Muhtasari wa Jumbe hizi ni Onyo kwamba Hukumu inayokuja kwa yule ambaye hamwabudu Mungu aliyeumba mbingu na nch jinsi alivyotoa maagizo Yeye Mwenyewe, na Kwamba adhabu hiyo itatolewa kwa wale wenye Ibada feki/bandia, wale wote wasiomwabudu inavyopaswa, watakunywa ghadhabu ya mvinyo isiyochanganywa kwa maji.

**11. Yohana Mbatizaji aliitwa Eliya wa siku zake kwa sababu (1)**
_____ Alipenda kuita moto kutoka mbinguni.
_____ Kuhani mkuu alilipendelea jina hilo.
_____ Mahubiri yake, kwa roho na nguvu za Eliya, yaliwatayarisha watu kwa ujio wa kwanza wa Yesu.

**12. Neno "injili" linamaanisha "habari njema." (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**Mungu Alichora Mipango - Somo la 17**

**Somo la 17**

Sote tunajua kwamba miaka 4,000 iliyopita, kwenye ncha ya kilele cha Mlima Sinai, Mungu alimpa Musa Amri Kumi. Lakini watu wengi hawajui kwamba wakati huo huo, Bwana alimpa Musa ramani za mojawapo ya miundo ya ajabu iliyowahi kujengwa - Patakatifu au Hekalu. Jambo hili lilikuwa la lazima yaani muhimu, kwa sababu Waisraeli hawangeweza kuingia katika Nchi ya Ahadi hadi  Madhabahu haya yakamilike kujenga. Hekalu hili la kipekee lililobebeka liliwakilisha maskani ya Mungu kati ya watu Wake, na huduma Zake zilionyesha taifa la watumwa waliowekwa huru panorama/mandhari tatu Za mpango wa wokovu. Kuchunguza kwa makini siri za Patakatifu kutaangaza uelewa wako wa jinsi ambayo Yesu anaokoa waliopotea na kuliongoza kanisa. Patakatifu pia ni ufunguo wa kuelewa unabii kadhaa. Mwongozo huu wa kupendeza wa Masomo unakuwezesha kuchunguza Patakatifu na kugundua maana zake zilizofichika. Matukio ya kusisimua yanakungoja ndugu mpendwa!

Mungu Mwenyewe alimpa Musa mipango ya patakatifu.

**1. Mungu alimwomba Musa ajenge nini?**
"Nao na wanifanyie patakatifu, ili nipate kukaa kati yao." Kutoka 25:8 .
**Jibu:** Bwana alimwomba Musa ajenge patakatifu, jengo maalum ambalo lingetumika kama makao ya Mungu mkuu wa mbinguni.

Maelezo Mafupi ya Patakatifu
Patakatifu palikuwa ni jengo la kifahari, la aina ya hema (15' x 45' lenye msingi wa dhiraa ya inchi 18) ambapo uwepo wa Mungu usio wa kawaida uliishi na huduma maalum zilifanywa.

Kuta hizo zilitengenezwa kwa mbao za mshita zilizosimama wima (za mbao), zilizowekwa katika vikalio vya fedha na kufunikwa kwa dhahabu ( Kutoka 26:15-19 , 29 ). Paa hiyo ilitengenezwa kwa tabaka nne za vifuniko: kitani, manyoya ya mbuzi, ngozi ya kondoo dume, ngozi ya pomboo ( Kutoka 26:1 , 6-14 ). Ilikuwa na vyumba viwili: Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu. Pazia nene, nzito au pazia ilitenganisha vyumba. Ua, eneo lililozunguka patakatifu, lilikuwa 75' x 150' ( Kutoka 27:18 ). Ilizungushiwa uzio wa nguo ya kitani nzuri iliyotegemezwa na nguzo 60 za shaba ( Kutoka 27:9-16 ).

**2. Mungu alitarajia watu wake wajifunze nini kutoka katika Patakatifu?**
"Ee Mungu, njia yako i katika Patakatifu; ni nani aliye Mungu mkuu kama Mungu wetu?" Zaburi 77:13 .

**Jibu:** Njia ya Mungu, au mpango wa wokovu, unafunuliwa katika Patakatifu pa duniani. Biblia inafundisha kwamba kila kitu katika Patakatifu au kilichounganishwa na huduma Yake kilikuwa ishara ya kitu ambacho Yesu angefanya katika kutuokoa. Hii ina maana kwamba hatuwezi kufahamu kikamilifu mpango wa wokovu hadi

tuelewe ishara inayounganishwa na Patakatifu. Kwa hivyo, umuhimu wa Mwongozo huu wa Utafiti hauwezi kuelezewa vya kutosha (Ni Muhimu sana).

Patakatifu na huduma zake zilipaswa kuonyesha mpango wa wokovu.

**3. Musa alipata ramani za Patakatifu kutoka chanzo gani? Jengo lilikuwa kopi/nakala ya nini?**
“Basi neno kuu katika hayo tuliyolinena ndilo hili: Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, yeye aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni, mhudumu wa Patakatifu, na wa hema ya Kweli; ambayo Bwana aliiweka, wala si mwanadamu.” “Wanatumikiao mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni, kama Musa alivyoagizwa na Mungu, alipokuwa tayari kujenga hema; “ Waebrania 8:1 , 2 , 5 .
**Jibu:** Michoro ya Patakatifu na maelezo kamili ya ujenzi wake yalitolewa kwa Musa kwa Mungu. Mchoro ulikuwa ni nakala ya Patakatifu pa asili mbinguni (original), palikuwa kielelezo cha Patakatifu pa Musa.

**4. Ni samani gani zilizokuwa kwenye ua?**
**Jibu:** A. Madhabahu ya sadaka za kuteketezwa ambapo wanyama walitolewa dhabihu ilikuwa katika ua, ndani ya pale unapoingia tu kweny emlango wake ( Kutoka 27:1-8 ). Madhabahu hii iliwakilisha msalaba wa Kristo. Mnyama alimwakilisha Yesu, dhabihu yenyewe halisi, ile isiyo na kifani ( Yohana 1:29 ).

B. Birika, lililokuwa kati ya madhabahu na mlango wa Patakatifu, lilikuwa ni beseni kubwa la kuogea lililotengenezwa kwa shaba. Hapa makuhani waliosha mikono na miguu kabla ya kutoa dhabihu au kuingia Patakatifu ( Kutoka 30:17-21) 38:8 ).

Maji yaliwakilisha utakaso kutoka kwa dhambi, au kuzaliwa upya, (au twaweza kusema ubatizo pia) ( Tito 3:5 ).

**5. Ni samani gani zilizokuwa mahali Patakatifu?**
**Jibu:** A. Meza ya mikate ya wonyesho ( Kutoka 25:23-30 ) iliwakilisha Yesu, Mkate wa mbinguni, Mkate wa uzima yaani ulio hai ( Yohana 6:51 ).

B. Kinara cha matawi saba ( Kutoka 25:31-40 ) kilimwakilisha Yesu, nuru ya ulimwengu ( Yohana 9:5). 1:9 ). Mafuta yalimwakilisha Roho Mtakatifu ( Zekaria 4:1-6). Ufunuo 4:5 ).

C. Madhabahu ya uvumba ( Kutoka 30:7 , 8 ) iliwakilisha maombi ya watu wa Mungu ( Ufunuo 5:8 ).

Kiti cha Rehema kinawakilisha kiti cha enzi cha Mungu mbinguni, ambacho pia kiko kati ya malaika wawili.

**6. Ni samani gani zilizokuwa mahali Patakatifu sana?**
**Jibu:** Sanduku la agano, samani pekee katika Patakatifu pa Patakatifu ( Kutoka 25:10-22 ), lilikuwa Sanduku la Agano au sanduku la mti wa mshita lililofunikwa

kwa dhahabu. Juu ya kifua walikuwa wamesimama malaika wawili waliotengenezwa kwa dhahabu ngumu. Kati ya malaika hawa kulikuwa na Kiti cha Rehema ( Kutoka 25:17-22 ), ambapo uwepo wa Mungu ulikaa.
Hii ilifananishwa na kiti cha enzi cha Mungu mbinguni, ambacho pia kiko kati ya malaika wawili
(Zaburi 80:1 ).

Amri Kumi zilikuwa ndani ya Sanduku la Agano nazo Zinawakilisha tabia ya Mungu, ambayo anaiweka ndani ya watu Wake.

**7. Ni nini kilikuwa ndani ya Sanduku la Agano?**

**Jibu:** Amri Kumi, ambazo Mungu aliziandika kwenye mbao za mawe kwa kidole cZhake, na ambazo watu Wake watazitii daima ( Ufunuo 14:12 ), hizi zilikuwa ndani ya sanduku ( Kumbukumbu la Torati 10: 4 , 5 ). Lakini kiti cha rehema kilikuwa juu yake, ambayo iliashiria kwamba maadamu watu wa Mungu waliungama na kuacha dhambi ( Mithali 28:13 ), rehema ingetolewa kwao kupitia damu ambayo ilinyunyizwa juu ya Kiti cha Rehema na kuhani ( Mambo ya Walawi 16:16; 15 , 16 ). Damu ya mnyama inawakilisha damu ya Yesu iliyomwagika kwa ajili yetu ili kutuletea msamaha wa dhambi ( Mathayo 26:28 ; Waebrania 9:22 ). Madhabahu ya Kuteketeza iinawakilisha Msalaba, au Dhabihu aliyoitoa iliyotolewa ilimwakilisha Mwana-Kondoo wa Mungu

Kwa maneno mengine wanyama waliotolewa dhabihu walimwakilisha Yesu, ambaye alitoa maisha Yake kwa ajili ya watu wote.

**8. Kwa nini wanyama walihitaji kutolewa dhabihu katika ibada za Patakatifu pa Agano la Kale?**
"Na katika torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu; na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo." Waebrania 9:22 . "Kwa maana hii ndiyo damu Yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi." Mathayo 26:28 .
**Jibu:** Dhabihu ya wanyama ilikuwa muhimu ili kuwasaidia watu kuelewa kwamba bila kumwaga damu ya Yesu, dhambi zao hazingeweza kusamehewa. Ukweli mbaya na wa kushangaza ni kwamba adhabu ya dhambi ni kifo cha milele ( Warumi 6:23 na Warumi 3:23). Kwa kuwa sisi sote tumefanya dhambi, sote tunapaswa kufa. Adamu na Hawa walipofanya dhambi, wangekufa mara moja isipokuwa Yesu, Ndiye ambaye aliitikia kwa kujitolea kutoa uhai Wake mkamilifu kuwa dhabihu ili kulipa adhabu ya kifo kwa watu wote ( Ufunuo 13:8 ) . Baada ya dhambi, Mungu alimtaka mwenye dhambi kuleta dhabihu ya mnyama ( Mwanzo 4:3-7 ). Mwenye dhambi alipaswa kuua mnyama kwa mkono wake mwenyewe ( Mambo ya Walawi 1:4 , 5). Damu ilileta mshtuko kwa mtu alipoona mnyama akichuruzika damu yaani yule mtu aliyemchinja na aliyetenda dhambi. Na ilimchoma moyo sana mwenye dhambi kwani uhalisi ulikuwa mzito kwa hayo matokeo mabaya ya dhambi (kifo cha milele) naye aliona hitaji lake kubwa la Mwokozi, na kwamba Yesu amekuwa mbadala wake. Bila Mwokozi, hakuna mtu aliyekuwa na tumaini lolote la wokovu siku zile na sasa pia.

Mfumo wa dhabihu ulifundisha, kupitia ishara ya mnyama aliyechinjwa, kwamba

Mungu angemtoa Mwanawe afe kwa ajili ya dhambi zao ( 1 Wakorintho 15:3 ). Yesu angekuwa sio tu Mwokozi wao, bali pia mbadala wao ( Waebrania 9:28 ). Yohana Mbatizaji alipokutana na Yesu, alisema, Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Yohana 1:29 . Katika Agano la Kale, watu walitazamia msalaba kwa ajili ya wokovu. Hata leo sisi Tunatazama nyuma Kalvari kwa wokovu. **Hakuna chanzo kingine cha wokovu** ( Matendo 4:12 ).

Dhabihu za wanyama zilifundisha Kweli yenye kushtua kwamba dhambi ingegharimu kifo cha Yesu.

**9. Je, Wanyama walitolewa dhabihu kwa jinsi gani katika utumishi wa Patakatifu, na jambo hilo lilikuwa na maana gani?**
"Naye ataweka mkono wake juu ya kichwa cha hiyo sadaka ya kuteketezwa; nayo itakubaliwa kwake, ili kufanya upatanisho kwa ajili yake." "Naye atamchinja upande wa madhabahu upande wa kaskazini." Mambo ya Walawi 1:4 , 11 .

**Jibu:** Mtenda dhambi alipoleta mnyama wa dhabihu kwenye mlango wa ua, kuhani alimpa kisu na beseni. Mwenye dhambi aliiweka mikono yake juu ya kichwa cha mnyama na kuungama dhambi zake. Hii iliashiria uhamisho wa dhambi kutoka kwa mwenye dhambi hadi kwa mnyama. Wakati huo, mtenda dhambi alichukuliwa kuwa hana hatia na mnyama kuwa na hatia. Kwa kuwa sasa mnyama huyo alikuwa na hatia kwa njia ya mfano, ilimbidi kulipa mshahara wa dhambi—kifo. Mtenda dhambi alimwegemea mnyama na kumchinja, Kwa kumchinja mnyama huyo kwa mkono wake mwenyewe, mtenda-dhambi huyo alifundishwa waziwazi kwamba dhambi ilisababisha kifo cha mnyama asiye na hatia na kwamba dhambi yake ingesababisha kifo cha Yesu asiye na hatia.

**10. Mnyama wa dhabihu alipotolewa kwa ajili ya kutaniko lote, kuhani alifanya nini kwa damu? Je, hii inaashiria nini?**
"Na kuhani aliyetiwa mafuta ataleta baadhi ya damu ya ng'ombe na kuileta ndani ya hema ya kukutania; kisha kuhani atatia kidole chake katika hiyo damu, na kuinyunyiza mara saba mbele za Bwana, mbele ya pazia." Mambo ya Walawi 4:16, 17.

**Jibu:** Wakati dhabihu ilipotolewa kwa ajili ya dhambi za kusanyiko lote, damu ilichukuliwa na kuhani, ambaye alimwakilisha Yesu ( Waebrania 3:1 ), ndani ya Patakatifu na kunyunyiziwa mbele ya pazia lililotenganisha vyumba viwili. Uwepo wa Mungu ulikaa upande wa pili wa pazia. Kwa hivyo, dhambi za watu ziliondolewa na kuhamishiwa kwa njia ya mfano kwenye Patakatifu. Huduma hii ya damu ya kuhani ilifananisha huduma ya sasa ya damu ya Yesu kwa ajili yetu mbinguni. Baada ya Yesu kufa msalabani kama dhabihu yetu kwa ajili ya dhambi, alifufuka na kwenda mbinguni kama Kuhani wetu kuhudumu damu Yake katika Patakatifu pa mbinguni ( Waebrania 9:11 , 12 ). Damu inayohudumiwa na kuhani wa kidunia inawakilisha Yesu akitumia damu Yake kwenye kumbukumbu zetu za dhambi katika Patakatifu pa Patakatifu, ikionyesha kwamba hizo dhambi zimesamehewa tunapoziungama katika Jina Lake ( 1 Yohana 1:9 ) .

Kama dhabihu yetu, Yesu hutuletea maisha yaliyobadilishwa kabisa na dhambi zote zimesamehewa.

**11. Kulingana na huduma za Patakatifu, ni katika nafasi gani kuu mbili ambazo Yesu hutumikia watu Wake? Je! ni faida gani za ajabu tunazopokea kutoka kwa huduma Yake ya upendo?**

"Kristo pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka kwa ajili yetu." 1 Wakorintho 5:7 . "Basi, kwa kuwa tunaye Kuhani Mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa maana hatuna Kuhani Mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie Kiti cha Neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji." Waebrania 4:14-16 .

**Jibu:** Yesu anatumika kama dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu na kama Kuhani wetu wa mbinguni. Kifo cha Yesu kama Mwana-Kondoo wa dhabihu na mbadala, na huduma Yake yenye nguvu inayoendelea kama Kuhani wetu wa mbinguni, inatimiza miujiza miwili ya ajabu kwetu:

A. Badiliko kamili la maisha linaloitwa kuzaliwa upya, na dhambi zote za zamani zimesamehewa ( Yohana 3). 3-6 Warumi 3:25 ).

B. Uwezo wa kuishi wakati uliopo na ujao ( Tito 2:14). Wafilipi 2:13 ).

Miujiza hii miwili humfanya mtu kuwa mwadilifu- maana yake kuna uhusiano sahihi kati ya mtu na Mungu. Hakuna njia iwezekanayo ya mtu kuwa mwenye haki kwa matendo (juhudi zake mwenyewe), kwa sababu haki inahitaji miujiza ambayo ni Yesu pekee awezaye kutimiza ( Matendo 4:12 ). Mtu anakuwa mwadilifu kwa kumwamini Yesu kumfanyia yale ambayo hawezi kujifanyia mwenyewe. Hiki ndicho kinachomaanishwa na Neno la kibiblia "haki kwa imani." Ninamwomba Yesu awe mtawala wa maisha yangu na kumwamini Yeye kufanya miujiza inayohitajika ninaposhirikiana Naye kikamilifu. Haki hii, ambayo imetimizwa kimiujiza kwangu na ndani yangu na Yesu, ndiyo haki pekee ya Kweli iliyopo. Kila aina nyingine ni bandia.
Yesu, kwa miujiza yake, atatufanya kwa furaha tu kufanya mambo yanayompendeza Mungu.

**12. Ni ahadi gani sita kuu ambazo Biblia inatupa kuhusu haki inayotolewa kwetu kupitia Yesu?**

**Jibu:**
A. Atazifunika dhambi zetu zilizopita na kutuhesabu kuwa hatuna hatia ( Isaya 44:22 Yohana 1:9 ).

B. Tuliumbwa kwa mfano wa Mungu hapo mwanzo ( Mwanzo 1:26 , 27). Yesu anaahidi kuturudisha kwa mfano wa Mungu ( Warumi 8:29 ).

C. Yesu anatupa shauku ya kuishi kwa haki na kisha hutujalia nguvu zake za kuitimiza ( Wafilipi 2:13 ).
D. Yesu, kwa miujiza Yake, atatufanya tufanye kwa furaha tu mambo yanayompendeza Mungu ( Waebrania 13:20-21 , Yohana 15:11 ).

E. Anaondoa hukumu ya kifo kutoka kwetu kwa kutuhesabia maisha Yake yasiyo na dhambi na kifo cha upatanisho ( 2 Wakorintho 5:21 ).

F. Yesu anachukua jukumu la kutuweka waaminifu hadi atakaporudi kutuchukua mbinguni ( Wafilipi 1:6). Yuda 1:24 ).

Yesu Yuko tayari kutimiza ahadi hizi zote tukufu maishani mwako. Uko tayari? Piga magoti sasa na umwombe ayatawale maisha yako. Yeye hatakuangusha.
Jukumu letu katika wokovu ni kufuata kwa upendo na kwa hiari pale Yesu anapotuongoza.

**13. Je, mtu ana nafasi yoyote ya kufanya katika kuwa mwenye haki kwa imani?**
"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni." Mathayo 7:21 .

**Jibu:** Ndiyo, Yesu anasema ni lazima tufanye mapenzi ya Baba Yake. Katika siku za Agano la Kale, mtu ambaye kweli alikuwa ameongoka aliendelea kuleta wana-kondoo kwa dhabihu, akionyesha huzuni yake kwa ajili ya dhambi na hamu yake ya moyo yote ya kumwacha Bwana aongoze kabisa maishani mwake.

Leo, ingawa hatuwezi kufanya miujiza inayohitajika ili kuwa wenye haki, ni lazima kila siku tujikabidhi kwa Yesu ( 1 Wakorintho 15:31 ), tukimualika atawale maisha yetu ili miujiza hiyo itendeke. Ni lazima tuwe tayari kuwa watiifu na kufuata kila mahali Yesu anapotuongoza ( Yohana 12:26). Isaya 1:18-20 ).

Dhambi hutufanya sisi kutaka kuwa na njia zetu wenyewe ( Isaya 53:6 ) na, hivyo, kuasi dhidi ya Bwana kama Shetani alivyofanya hapo mwanzo ( Isaya 14:12-14 ). Kumruhusu Yesu atawale maisha yetu nyakati fulani ni jambo gumu sana kama vile kung'olewa jicho au mkono uliong'olewa ( Mathayo 5:29 , 30 ), kwa sababu dhambi ni yenye kulewa na inaweza kushindwa tu na nguvu za kimuujiza za Mungu ( Marko 10:27 ) .

Wengi wanaamini kwamba Yesu atawachukua wote wanaodai kuwa wameokoka na kuwapeleka mbinguni, bila kujali mwenendo wao. Lakini hii sivyo. Ni uzushi wa Shetani. Mkristo lazima afuate mtindo wa maisha wa Yesu ( 1 Petro 2:21 ). Damu yenye nguvu ya Yesu inaweza kutimiza hili kwa ajili yetu sisi sote ( Waebrania 13:12), lakini tu ikiwa tunampa Yesu awe mtawala kamili wa maisha yetu na kufuata kwa furaha anakoongoza, ingawa njia inaweza kuwa ya mawe na ngumu wakati mwingine ( Mathayo 7 : 13 , 14 , 21 ).

Mbuzi wa Bwana aliwakilisha Yesu, ambaye angekufa kwa ajili ya dhambi zetu.

**14. Unaweza kunisaidia kuelewa siku ya upatanisho?**

**Jibu:** A. Mara moja kila mwaka, siku ya upatanisho, siku kuu ya hukumu ilifanyika katika Israeli ( Mambo ya Walawi 23:27 ). Wote walipaswa kuungama kila dhambi. Wale waliokataa siku hiyohiyo walikatiliwa mbali kabisa na kambi ya Israeli ( Mambo ya Walawi 23:29 ).

B. Mbuzi wawili walichaguliwa: Mmoja, mbuzi wa Bwana na mwingine, mbuzi wa Azazeli, akiwakilisha Shetani (Mambo ya Walawi 16:8 ). Mbuzi wa Bwana alichinjwa na kutolewa sadaka kwa ajili ya dhambi za watu ( Mambo ya Walawi 16:9). Lakini siku hii damu ilichukuliwa hadi Patakatifu pa Patakatifu na kunyunyiziwa juu na mbele ya Kiti cha Rehema ( Mambo ya Walawi 16:14 ). Siku hii ya pekee ya hukumu ndiyo kuhani mkuu aliingia Patakatifu pa Patakatifu ili kukutana na Mungu kwenye Kiti cha Rehema.

Damu ya kunyunyiziwa (iliyowakilisha dhabihu ya Yesu) ilikubaliwa na Mungu, na dhambi zilizoungamwa za watu zilihamishwa kutoka Patakatifu hadi kwa kuhani mkuu. Kisha alihamisha dhambi hizi zilizoungamwa kwa mbuzi wa Azazeli, ambaye aliongozwa hadi jangwani ( Mambo ya Walawi 16:16 , 20-22 ). Kwa namna hii, Patakatifu palitakaswa dhambi za watu, ambazo zilikuwa zimehamishiwa pale kwa damu iliyonyunyiziwa mbele ya pazia na zilikuwa zikikusanywa/zikirundikana kwa mwaka mmoja.

Siku ya upatanisho ya Israeli ilikuwa ishara ya hukumu ya mwisho, ambayo ingesuluhisha swali la dhambi milele katika ulimwengu wote.

**15. Je, siku ya upatanisho inaashiria au kuonyesha alama ya sehemu ya mpango mkuu wa Mungu wa wokovu, kama zilivyofanya sehemu nyingine za Patakatifu pa kidunia na huduma zake?**
“Basi ilikuwa sharti mifano ya mambo yaliyo mbinguni yasafishwe kwa hizo; bali mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo. Waebrania 9:23 .

**Jibu:** Ndiyo. Ibada za siku hiyo zilielekeza kwenye kufutwa kwa dhambi na Kuhani Mkuu halisi katika Patakatifu pa mbinguni. Kupitia damu Yake iliyomwagwa iliyotumiwa kwa wale walioandikwa katika kitabu cha uzima, Kristo angethibitisha maamuzi ya watu Wake ya kumtumikia Yeye milele. Siku hii maalum ya hukumu, kama ile ya Yom Kippur ya Israeli, ilionyesha upatanisho wa mwisho utakaofanywa kwa ajili ya sayari ya Dunia. Kutokana na aina ya kila mwaka ya siku ya kale ya upatanisho, wanadamu wote wanahakikishiwa kwamba Kuhani wetu Mkuu mwaminifu, Yesu, angali mpatanishi mbinguni kwa ajili ya watu Wake na Yuko tayari kufuta dhambi za wote ambao watakuwa na imani katika damu Yake iliyomwagwa. Upatanisho wa mwisho unaongoza kwenye hukumu ya mwisho, ambayo inasuluhisha swali la dhambi katika maisha ya kila mtu, na kufikia kilele chake katika maisha au kifo.

**Matukio Muhimu**

Utagundua katika Masomo mawili ambayo yanafuata jinsi mfano wa Patakatifu pa duniani na hasa siku ya upatanisho ulivyofananisha na matukio muhimu ya wakati wa mwisho, ambayo Mungu ataleta kutokea katika Patakatifu pa mbinguni. Madhabahu ni wokovu katika picha ili tuweze kuelewa vyema.

**Tarehe ya Hukumu**
Katika Mwongozo unaofuata wa Mafunzo, tutachunguza unabii muhimu wa Biblia ambapo Mungu anaweka tarehe ya kuanza kwa hukumu ya mbinguni. Hakika kisa hiki kinasisimua kwa kweli!

**16. Niko tayari kukubali haki ya Kristo, ambayo inajumuisha msamaha, kusafishwa kutoka kwa dhambi, na uwezo wa kuishi katika wakati uliopo na ujao.**

**Jibu:**

**Maswali au Kwizz**
**1. Ni samani gani zilizokuwa kwenye ua wa Patakatifu? (2)**
_____ Kiti cha Rehema.
_____ Birika.
_____ Viti.
_____ Madhabahu ya sadaka za kuteketezwa.

**2. Uwepo wa Mungu ulikaa kwenye kiti cha rehema. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**3. Kinara cha matawi saba kiliwakilisha (1)**
_____ Yesu, nuru ya ulimwengu.
_____ Ujio wa pili wa Kristo.
_____ Kuta zinazometa za Yerusalemu mpya.

**4. Kusudi la Patakatifu na huduma zake lilikuwa ni (1)**
_____ Kuwasaidia watu kuelewa malaika.
_____ Wape watu chakula cha nyama.
_____ Alama ya mpango wa wokovu.

**5. Ni nani aliyechora mipango ya Patakatifu? (1)**
_____ Nuhu
_____ Malaika.
_____ Haruni.
______Mungu.

**6. Amri Kumi zilikuwa ndani ya Sanduku la Agano. (1)**

_____ Ndiyo.
_____   Hapana.

**7. Wanyama wa dhabihu waliochinjwa waliwakilisha (1)**
_____ Roho Mtakatifu.
_____ Vita.
_____ Yesu.

**8. Kulingana na Patakatifu, Yesu anatutumikia/anatuhudumia katika nafasi zipi mbili? (2)**
_____ Mfalme.
_____ Sadaka.
_____ Kuhani Mkuu.
_____ Mtawala wa ulimwengu.

**9. Ni lipi kati ya haya lililokuwa kweli kuhusu Patakatifu pa kidunia? (2)**
_____ Ilikuwa na vyumba vitatu.
_____ Ilikuwa muundo wa aina ya hema.
_____ Ukubwa wake ulikuwa 500' x 1000'.
_____ Ua ulitengenezwa kwa nguzo za shaba na nguo ya kitani.
_____ Paa lilitengenezwa kwa vigae vya Misri.
_____ Birika lilikuwa katika Patakatifu pa Patakatifu.

**10. Haki kwa imani ndiyo haki pekee ya Kweli. (1)**
_____ Ndiyo.
_____   Hapana.

**11. Haki kwa imani hutokana na (1)**
_____ Matendo ya mwanadamu.
_____Kubatizwa.
_____ Imani katika Yesu Kristo pekee.

**12. Ni nani aliyemwua mnyama wa dhabihu aliyeletwa na mwenye dhambi? (1)**
_____ Mungu.
_____ Kuhani.
_____ Mwenye dhambi.

**13. Ni maneno gani ambayo ni ya kweli kuhusu uadilifu ambao Yesu hutoa? (3)**
_____ Itaturudisha kwa mfano wa Mungu.
_____ Sio muujiza.
_____ Matendo yetu mema ni sehemu kubwa yake.
_____ Inafunika dhambi zetu zilizopita.
_____ Inatupa hamu ya kuishi sawa.

**14. Ni yapi kati ya yafuatayo ni ya kweli kuhusu siku ya upatanisho? (4)**

_____ Ilifanyika kila mwezi.
_____ Ilikuwa siku ya hukumu.
_____ Ilikuwa siku ya michezo na furaha nzuri.
_____ Iliashiria hukumu ya mwisho.
_____ Mbuzi wa Azazeli alifananisha Shetani.
_____ Damu ilichukuliwa hadi mahali Patakatifu sana.

**15. Haki maana yake ni uhusiano mzuri na Mungu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**16. Kuua mnyama kulisaidia watu kutambua kwamba dhambi ilileta hukumu ya kifo juu ya watu wote. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**Kwa Wakati Sahihi! Miadi ya Kinabii Yafichuliwa!**

**Somo la 18**

Funga mkanda wako wa kiti ( weka seatbelt)! Sasa tunaanza kuuchunguza unabii wa muda mrefu zaidi katika Biblia - unabii uliotabiri kwa ukamilifu ujio wa kwanza wa Yesu na wakati wa kifo Chake. Katika Mwongozo wa Kusoma 16, "Ujumbe wa Malaika kutoka Angani," Tulijifunza kwamba Mungu ana ujumbe muhimu sana ambao ulimwengu wote lazima usikie kabla ya kurudi kwa Kristo! Jambo la kwanza linaamuru watu kumwabudu Mungu na kumtukuza, kwa sababu saa ya hukumu Yake imefika ( Ufunuo 14:7 ). Katika Danieli 8 na 9, Mungu anafunua tarehe ya hukumu Yake ya mwisho kuanza na vidokezo vya unabii vyenye nguvu na vinavyomthibitisha Kristo kama Masihi. Hivyo hakuna unabii katika Maandiko yote ulio muhimu zaidi kama huu - lakini ni watu wachache tu wanaoufahamu! Wengine wanautafsiri vibaya kabisa. Tafadhali soma Danieli sura ya 8 na 9 kabla ya kuanza Mwongozo huu wa Somo, na umwombe Roho wa Mungu akuongoze katika kuelewa somo hili la ajabu.

**Kondoo mume anawakilisha Umedi na Uajemi.**
**1. Katika maono, Danieli aliona kondoo mume mwenye pembe mbili akisogea mbele na kusukuma pembe zake magharibi, kaskazini, na kusini na kumshinda kila mnyama aliyekutana naye (Danieli 8:3, 4). Kondoo huyo anaashiria nini?**

"Yule kondoo mume uliyemwona mwenye pembe mbili ndiye wafalme wa Umedi na Uajemi." Danieli 8:20 .
**Jibu:** Kondoo dume ni mfano wa ufalme uliotawala dunia, ufalme wa Umedi na Uajemi, ambao pia uliwakilishwa na dubu katika unabii wa Danieli 7:5 . Unabii wa vitabu vya Biblia vya Danieli na Ufunuo hufuata kanuni ya "rudia tenakueleza na Upanue zaidi kwa maelezo unapourudia yaani repeat and expand," ambayo

humaanisha kwamba unarudia unabii uliotajwa katika sura za awali za kitabu hicho na kuupanua. Mbinu hii huleta uwazi na uhakika wa unabii wa Biblia (Sura zinazofanana za unapii na kuupanua zaidi ni Daniel 2, 7 na 8/9).

Mbuzi anaashiria Ugiriki.

**2. Danieli aliona mnyama gani mwenye kuvutia baadaye?**
"Na yule beberu ni mfalme wa Ugiriki, na ile pembe kubwa iliyo katikati ya macho yake ndiye mfalme wa kwanza. Sasa ile iliyovunjika, na ambapo nne zilisimama kwa ajili yake, falme nne zitasimama katika taifa hilo." Danieli 8:21, 22 .
**Jibu:** Kisha katika maono ya Danieli, mbuzi-dume mwenye pembe moja kubwa akatokea ghafula, akisafiri kwa kasi kubwa. Naye akamshambulia na kumshinda kondoo dume. Kisha ile pembe kubwa ikakatwa na pembe nne zikatokea mahali pake. Mbuzi-dume mkali anafananishwa na ufalme wa tatu uliotawala ulimwengu wa Ugiriki, na ile pembe kubwa ilifananishwa na ***Aleksanda Mkuu au Aleksanda wa Makedonia.*** Pembe nne zilizochukua nafasi ya ile pembe kubwa zinawakilisha falme nne ambazo milki ya Aleksanda iligawanywa baada ya yeye kufa akiwa kijana. Katika Danieli 7:6 , falme hizi nne zinawakilishwa na vichwa vinne vya mnyama chui, ambaye pia anafananishwa na Ugiriki. Ishara hizi zinafaa sana kwanini rahisi kuzitambua katika historia, yaani hata ukisoma historia hiyo ya kale leo, nembo hizi zinatumika.

| **MKOA** | **JUMLA** |
|---|---|
| **I. Makedonia**<br>*(Makedonia ilitawala Ugiriki kwa miaka 200.)* | **Cassander** |
| **II. Asia**<br>*(Inaitwa Asia Ndogo leo. Ni Uturuki ya kisasa.)* | **Lysimachus - Uongo sim cus**<br>*(kwa ujumla ilitawala sehemu ya magharibi ya Asia Ndogo pamoja na Thrace huko Ulaya.)* |
| **III. Syria** | **Seleuchus -**<br>*(pamoja na sehemu za Asia.)* |
| **IV. Misri** | **Ptolemy**<br>*(Kleopatra mwenye sifa mbaya alikuwa Ptolemy wa mwisho kutawala Misri.)* |

"Pembe ndogo" ya Danieli sura ya 8 inawakilisha Rumi katika hatua zake zote za kipagani na za kipapa. Kwa hiyo pembe ndogo ya siku za mwisho ni upapa.

**3. Kulingana na Danieli 8:8, 9 , nguvu ya pembe ndogo baadaye ikatokea. Pembe ndogo inawakilisha nini?**

**Jibu:** Pembe **ndogo inawakilisha Rumi** . Wengine wamependekeza kwamba pembe ndogo inawakilisha ***Antiochus Epiphanes*** , mfalme wa ***Seleucid*** ambaye alitawala ***Palestina*** katika karne ya pili KK na ambaye alivuruga ibada za

Kiyahudi. Wengine, huweka ndani viongozi wengi wa Matengenezo ya Kanisa, wameamini kwamba ile pembe ndogo inawakilisha Roma katika sura zake za kipagani na za kipapa. Hebu tuchunguze ushahidi wa wazi wa Biblia kwa hili:

A. Kwa kupatana na kanuni ya kinabii ya "rudia na kupanua," Rumi lazima iwe mamlaka inayowakilishwa hapa kwa sababu sura zote mbili za 2 na 7 za Danieli zinaelekeza Rumi kama ufalme unaofuata Ugiriki. Danieli 7:24-27 pia inathibitisha ukweli kwamba Rumi katika hali yake ya upapa itafuatiwa na ufalme wa Kristo. Pembe ndogo ya Danieli sura ya 8 inalingana na mpangilio huu haswa: Inafuata Ugiriki na hatimaye inaharibiwa kwa njia isiyo ya kawaida au "kuvunjwa bila mkono" katika ujio wa pili wa Yesu. (Linganisha Danieli 8:25 na Danieli 2:34 .)

B. Danieli sura ya 8 inasema Wamedi na Waajemi wangekuwa "wakuu" ( mstari wa 4 ), Wagiriki "wakuu sana" ( mstari wa 8 ), na ile mamlaka ya pembe ndogo " kubwa sana" (mstari 9). Historia iko wazi kwamba hakuna mamlaka iliyofuata Ugiriki ikawa "kuu kupita" zaidi ya Roma. Mambo yote haya yamo kwenye historia ya ulimwengu pia, tumeyasoma wengi wetu madarasani, na pia unaweza kuyapata kwenye mtandao, google au injini zingine za kutafuta au kusachi, kwa maneno kama vile " History of Kingdoms that ruled the world"

C. Rumi ilipanua mamlaka yake hadi kusini (Misri), mashariki (Makedonia), na "nchi ya kupendeza" (Palestina) sawasawa na unabii ulivyotabiri (mstari wa 9). Hakuna mamlaka kuu zaidi ya Rumi inayolingana na hatua hii.

D. ***Ni Rumi pekee iliyosimama dhidi ya Yesu, "mkuu wa jeshi"*** (mstari wa 11) na ***"Mfalme wa wakuu"*** (Kifungu cha 25). ***Rumi ya kipagani ilimsulubisha Yesu, na Ndiyo ilitawala wakati Yeye alizaliwa.*** Pia iliharibu hekalu la Wayahudi. Na ***Rumiya upapa*** ilisababisha Patakatifu pa mbinguni ***"kutupwa chini"*** (mstari wa 11) na ***"kukanyagwa chini ya miguu"*** ( mstari wa 13 ) kwa kuchukua nafasi ya huduma muhimu ya Yesu, Kuhani wetu Mkuu mbinguni, na ukuhani wa kidunia unaodai kusamehe dhambi. Hakuna mtu ila Mungu awezaye kusamehe dhambi ( Luka 5:21 ). ***Na Yesu Ndiye Kuhani au Mpatanishi wetu pekee*** ( 1 Timotheo 2:5 ).

Ile mamlaka ndogo ya pembe ilitesa na kuharibu mamilioni ya watu wa Mungu.

**4. Danieli 8 inatufahamisha kwamba mamlaka hii ndogo ya pembe ingeangamiza watu wengi wa Mungu (mistari 10, 24, 25) na kutupa ile Kweli chini (mstari 12). Mtakatifu alipouliza watu wa Mungu na Patakatifu pa mbinguni pangekanyagwa kwa muda gani, jibu la mbinguni lilikuwa nini**
"Akaniambia, Hata siku elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa." Danieli 8:14 .

**Jibu:** Jibu la Mbingu lilikuwa kwamba +Patakatifu pa mbinguni pangetakaswa baada ya siku 2,300 za kinabii, au miaka 2,300 halisi. ( Mwongozo wa Somo la 15 unatoa ufafanuzi kamili wa kanuni ya kinabii ya siku ni mwaka, inayopatikana katika Ezekieli 4:6 na Hesabu 14:34 .) Tayari tumejifunza kwamba utakaso wa

Patakatifu pa kidunia ulifanyika siku ya upatanisho. katika Israeli ya kale.

Siku hiyo watu wa Mungu walitambulishwa waziwazi kuwa Wake, na kumbukumbu ya dhambi zao iliondolewa. Waovu walioshikamana na dhambi walikatiliwa mbali na Israeli milele. Hivyo kambi ilisafishwa na dhambi.

Mbingu hapa zilikuwa zikimhakikishia Danieli kwamba dhambi na ile mamlaka ndogo ya pembe hazingeendelea kufanikiwa, wala kutawala ulimwengu, na kuwatesa watu wa Mungu milele. Badala yake, katika miaka 2,300 Mungu angeingilia kati siku ya upatanisho ya kimbingu, au hukumu, ambapo dhambi na watenda-dhambi wangetambuliwa na baadaye kuondolewa katika ulimwengu wote kabisa, milele. Hivyo ulimwengu utasafishwa na dhambi. Maovu dhidi ya watu wa Mungu yatarekebishwa hatimaye, na amani na upatanifu wa Edeni utajaa tena kwenye ulimwengu wote mzima.Danieli alisali kwamba Mungu amsaidie kuelewa ule unabii wa miaka 2,300.

**5. Malaika Gabrieli alikazia jambo gani la lazima mara kwa mara?**
"Fahamu, Ee mwanadamu; maana maono hayo yatakuwa wakati wa mwisho." "Nitakujulisha yatakayokuwa katika mwisho wa ghadhabu." "Basi, yafunge maono haya; maana yatakuwa ya siku nyingi." Danieli 8:17 , 19 , 26 , mkazo umeongezwa.
**Jibu:** Gabrieli alisisitiza mara kwa mara kwamba maono ya siku 2,300 yalihusisha matukio ya wakati wa mwisho, ambayo yalianza mwaka wa 1798, kama tulivyojifunza katika Mwongozo wa 15. Malaika alitaka tuelewe kwamba unabii wa siku 2,300 ni ujumbe ambao unatumika kimsingi. kwa sisi sote tunaoishi katika wakati wa mwisho wa historia ya dunia. Hili lina maana maalum kwetu leo.

**Utangulizi wa Danieli Sura ya 9**
Baada ya maono ya Danieli ya sura ya 8, malaika Gabrieli alikuja na kuanza kumweleza maono hayo. Gabrieli alipofikia hatua ya siku 2,300, Danieli alianguka na kuwa mgonjwa kwa muda. Alipata nguvu tena na kuanza tena kufanya kazi ya mfalme lakini alihangaikia sana sehemu ambayo haikuelezwa kwenye maono, yaani zile siku 2,300. Danieli alisali kwa bidii kwa ajili ya watu wake, yaani Wayahudi waliokuwa utumwani katika Umedi na Uajemi. Aliungama dhambi zake na kumsihi Mungu awasamehe watu Wake. Danieli sura ya 9 huanza na maombi ya dhati ya nabii ya kuungama na kusihi kwa Mungu.

Tafadhali chukua muda sasa kusoma Danieli 9 kabla ya kuendelea zaidi na Mwongozo huu wa Somo.
Malaika Gabrieli alikuja kwa Danieli ili kumweleza ule unabii wa miaka 2,300.

**6. Danieli alipokuwa akiomba, ni nani aliyemgusa ghafula na kwa ujumbe gani (Danieli 9:21-23)?**

**Jibu:** Malaika Gabrieli alimgusa na kusema kwamba amekuja kueleza maono mengine yote yaliyofafanuliwa katika Danieli sura ya 8 (linganisha Danieli 8:26 na Danieli 9:23 ).
Gabrieli alimweleza Danieli matukio muhimu ambayo yangetukia ndani ya ile

miaka 2,300.

**7. Ni kiasi gani kati ya siku 2,300 zingegawiwa (au kukatiliwa mbali kwa ajili ya) watu wa Danieli, Wayahudi, na jiji lao kuu, Yerusalemu ( Danieli 9:24 )?**
**Jibu:** Majuma sabini yalipaswa "kuamuliwa," au kukatiliwa mbali, kwa Wayahudi. Majuma sabini ya kinabii ni miaka 490 halisi (70 x 7 = 490). Watu wa Mungu wangerudi hivi karibuni kutoka uhamishoni kama mateka katika Umedi na Uajemi, na Mungu angekatilia mbali miaka 490 kutoka ile miaka 2,300 na kuwagawia watu Wake waliochaguliwa kuwa fursa nyingine ya kutubu na kumtumikia.

**8. Ni tukio gani na tarehe ambayo ingetia alama mahali pa kuanzia kwa unabii wa siku 2,300 na miaka 490 ( Danieli 9:25 )?**

**Jibu:** Tukio la kuanzia lilikuwa ni amri kutoka kwa Mfalme Artashasta wa Uajemi iliyowaruhusu watu wa Mungu (waliokuwa mateka katika Umedi na Uajemi) kurudi Yerusalemu na kujenga upya mji. Amri hiyo, inayopatikana katika Ezra sura ya 7, ilitolewa mwaka wa 457 KK--mwaka wa saba wa mfalme (mstari wa 7)--na ilitekelezwa katika majira ya vuli au majira ya kupukutisha majani yaani Autumn. Artashasta alianza utawala wake mwaka 464 KK
Ubatizo wa Yesu ulitimiza kwa usahihi unabii wa Biblia.


**9. Malaika alisema kwamba majuma 69 ya kinabii, au miaka 483 halisi (69 x 7 = 483), iliyoongezwa hadi 457 KK ingemfikia Masihi (Danieli 9:25). Je!**

**Jibu:** Ndiyo, kwa kweli! Hesabu hapa unapokorokotoa zinaonyesha unaposonga mbele miaka miaka 483 kutoka majira ya vuli ya mwaka 457 BC utafika kwenye majira ya vuli ya mwaka AD 27 Mwaka ambao Yesu alibatizwa au alisimikwa kuingia kazini. Neno **"Masihi"** linamaanisha **"mpakwa mafuta"** ( Yoh. 1:41 , pambizo). Yesu alipakwa mafuta kwa Roho Mtakatifu ( Matendo 10:38 ) wakati wa ubatizo Wake ( Luka 3:21, 22 ). Upako Wake ulifanyika katika mwaka wa 15 wa utawala wa Tiberio Kaisari ( Luka 3:1 ), ambayo ilikuwa AD 27. Na ni jambo la kushangaza kufikiria utabiri huo ulifanywa zaidi ya miaka 500 kabla na ukaenda kutimia kwa ukamilifu kabisa!

Kisha Yesu akaanza kuhubiri kwamba "wakati umetimia" (akimaanisha miaka 483 ambayo ingemfikia Masihi). Hivyo alithibitisha kwa sauti unabii huo ( Marko 1:14 , 15 Wagalatia 4:4 ). Kwa hiyo Yesu kwa kweli alianza huduma Yake kwa kurejelea waziwazi ule unabii wa siku 2,300, akikazia umuhimu na usahihi wake. Huu ni ushahidi wa kutisha, wa kutosha na wa kusisimua kwamba:

A. Biblia imevuviwa.

B Yesu ndiye Masihi



**10. Sasa tumemaliza kuchunguza miaka 483 ya ule unabii wa miaka 490. Sasa limesalia juma moja la kinabii, au miaka saba halisi (Danieli 9:26, 27). Nini kitatokea baadaye? Na kinatokea lini?**

**Jibu:** Yesu "anakatiliwa mbali" au kusulubishwa "katikati ya juma," ambayo ni miaka mitatu na nusu baada ya kutiwa mafuta Kwake, au kuchipua mimea yaani Spring ya mwaka 31 BK. Tafadhali angalia jinsi injili inavyofunuliwa katika mstari wa 26: "Baada ya majuma sitini na mawili Masihi atakatiliwa mbali, lakini si kwa ajili Yake Mwenyewe."

Hakika, asifiwe Mungu, Yesu alipokatiliwa mbali, haikuwa kwa ajili Yake Mwenyewe. Yeye "ambaye hakutenda dhambi" ( 1 Petro 2:22 ) alisulubishwa kwa ajili ya dhambi zetu ( 1 Wakorintho 15:3 ) Isaya 53:5 ). Uhai wa Yesu wenye thamani ulitolewa kwa upendo na kwa hiari ili kutuokoa sisi kutoka katika dhambi. Haleluya, ni Mwokozi wa namna gani Huyu! Dhabihu ya upatanisho ya Yesu ndiyo kiini hasa cha Danieli sura ya 8 na 9 .
Wanafunzi walihubiria umati wa Wayahudi.

**11. Kwa kuwa Yesu alikufa baada ya miaka mitatu na nusu, angewezaje basi "kuthibitisha agano na wengi" kwa miaka saba kamili ya mwisho, kama vile unabii wa Danieli 9:27 unavyoamuru?**

**Jibu:** Agano ni agano Lake lenye baraka la kuwaokoa watu kutoka katika dhambi zao ( Waebrania 10:16 , 17 ). Baada ya huduma Yake ya miaka mitatu na nusu kuisha, Yesu alithibitisha agano kupitia wanafunzi Wake ( Waebrania 2:3 ). Aliwatuma kwanza kwa taifa la Kiyahudi ( Mathayo 10:5 , 6 ), kwa sababu watu Wake waliochaguliwa walikuwa bado na miaka mitatu na nusu iliyosalia ya nafasi yao ya miaka 490 ya kutubu.
Baada ya kupigwa mawe kwa Stefano, wanafunzi walianza kuwahubiria watu wa mataifa.

**12. Kipindi cha miaka 490 cha fursa ya mwisho kwa taifa la Kiyahudi kilipoisha katika masika ya 34 BK, wanafunzi walifanya nini?**

**Jibu:** Walianza kuhubiri injili kwa watu wengine na mataifa ya ulimwengu ( Matendo 13:46 ). Stefano, shemasi mwadilifu, alipigwa mawe hadharani mwaka wa 34 BK. Tangu tarehe hiyo na kuendelea Wayahudi, kwa sababu walimkataa Yesu na mpango wa Mungu, hawakuwa tena watu wateule wa Mungu au taifa. Badala yake, sasa Mungu anahesabu watu wa mataifa yote wanaomkubali na kumtumikia kuwa Wayahudi wa kiroho. Hawa wamekuwa wateule Wake--"warithi sawasawa na ahadi." Wayahudi wa kiroho, bila shaka, wanajumuisha Wayahudi ambao kila mmoja anamkubali na kumtumikia Yesu ( Wagalatia 3:27-29 ; Warumi 2:28 , 29 ).
Hukumu ya uchunguzi ya Mungu inashuhudiwa na jeshi la mbinguni.

**13. Baada ya 34 BK, ni miaka mingapi ya unabii wa miaka 2,300 iliyobaki? Je, ni tarehe gani ndiyo ya mwisho ya unabii huo? Malaika alisema nini kingetokea katika tarehe hiyo (Danieli 8:14)?**

**Jibu:** Kulikuwa na miaka 1,810 iliyobaki (2,300 minus 490 = 1,810). Tarehe ya mwisho ya unabii ni 1844 (AD 34 + 1810 = 1844). Malaika alisema Patakatifu pa mbinguni pangetakaswa, au hukumu ya mbinguni itaanza. (Patakatifu pa duniani paliharibiwa mwaka wa 70 BK.) Tulijifunza katika Mwongozo wa 17 kwamba siku ya upatanisho ya mbinguni, au hukumu, ilipangwa kwa ajili ya wakati wa mwisho. Sasa tunajua kwamba tarehe ya mwanzo ni 1844. Mungu aliweka tarehe hii. Ni hakika kama tarehe 27 BK kwa Yesu kuwa Masihi. Watu wa Mungu wa nyakati za mwisho lazima wawe wanaitangaza tarehe na tukio hili ( Ufunuo 14:6 , 7 ).

Utasisimka na kufurahishwa kujifunza habari za hukumu hiyo katika Mwongozo wa 19. Katika siku za Nuhu, Mungu alisema kwamba hukumu ya Gharika ingetukia katika miaka 120 ( Mwanzo 6:3 ) na ikawa hivyo. Katika siku za Danieli, Mungu alisema kwamba hukumu Yake ya wakati wa mwisho ingeanza baada ya miaka 2,300 ( Danieli 8:14 ) na ikawa hivyo. Hukumu ya Mungu ya wakati wa mwisho imekuwa ikiendelea kufanya kazi tangu 1844. Yesu anapokuja haji kuhukumu watu tena, hukumu inakuwa imekwisha kufanyika, ila wakati huo utakuwa wa kutoa thawabu.

**Maana ya Upatanisho**

Neno la Kiingereza "atonement" awali lilimaanisha "at-one-ment" yaani, hali ya kuwa "at one" au kuwa na umoja katika makubaliano. Inaashiria maelewano ya uhusiano. Upatanifu kamili ulikuwepo awali katika ulimwengu wote mzima. Kisha Lusifa, malaika wa mbinguni mwenye kipaji (kama tulivyojifunza katika Mwongozo wa Somo 2), alimpinga Mungu na kanuni Zake za serikali. Theluthi moja ya malaika wa mbinguni walijiunga na uasi wa Lusifa ( Ufunuo 12:3 , 4 , 7-9 ).

Uasi huu dhidi ya Mungu na kanuni Zake za upendo unaitwa dhambi katika Biblia ( Isaya 53:6 1 Yohana 3:4 ). Inaleta maumivu ya moyo, kuchanganyikiwa, machafuko, misiba, tamaa, huzuni, usaliti, na uovu wa kila aina. Mbaya zaidi, adhabu yake ni kifo ( Warumi 6:23 ) ambacho hakuna ufufuo katika ziwa la moto ( Ufunuo 21:8 ). Dhambi huenea haraka nayo ni hatari zaidi kuliko aina hatari zaidi ya saratani. Iliuweka ulimwengu wenyewe hatarini.
Kwa hiyo Mungu alimtoa Lusifa na malaika zake kutoka mbinguni ( Ufunuo 12:7-9 ), na Lusifa akapokea jina jipya "Shetani," ambalo linamaanisha "adui." Malaika wake walioanguka sasa wanaitwa mapepo. Shetani aliwashawishi Adamu na Hawa, na hivyo dhambi ikawa juu ya wanadamu wote. Msiba wa kutisha ulioje! Mgogoro mkubwa kati ya wema na uovu ulikuwa umeanza, na uovu ulionekana kushinda. Hali ilionekana kutokuwa na matumaini.

Lakini, hapana! Yesu, Mwana wa Mungu na Mungu Mwenyewe ambaye alikuwa zaidi ya watu wote ambao wangeishi duniani kwa thamani, alikubali kuutoa uhai Wake ili kulipa adhabu ya kifo kwa kila mwenye dhambi ( 1 Wakorintho 5:7 ) . Kwa kukubali dhabihu Yake, wenye dhambi wangewekwa huru kutokana na hatia ya dhambi ( Warumi 3:25 ). Mpango huu wa utukufu pia ulijumuisha Yesu kuingia katika maisha ya mtu pale Anapoalikwa na yule mtu ( Ufunuo 3:20 ) na kumbadilisha kuwa mtu mpya ( 2 Wakorintho 5:17 ). Ulitoa nguvu kutoka kwa Yesu ili kumpinga Shetani na kurejesha kila mtu aliyeongoka kwa mfano wa Mungu, ambaye aliumbwa kwa Mfano Wake ( Mwanzo 1:26 , 27 ; Warumi 8:29 ).

Sadaka hii ya upatanisho iliyobarikiwa inajumuisha mpango wa kutenga dhambi na kuiharibu ikiwa ni pamoja na Shetani na malaika zake walioanguka, pamoja na wote wanaojiunga naye katika uasi ( Mathayo 25:41 ; Ufunuo 21:8 ). Zaidi ya hayo, habari kamili kuhusu Yesu na serikali Yake yenye upendo na Shetani na udikteta wake wa kishetani itapelekwa kwa kila mtu duniani ili wote waweze kufanya uamuzi wenye akili na wenye ujuzi wa kujipatanisha na Kristo au Shetani ( Mathayo 24:14; Ufunuo 14:14 ; 6 , 7 ).

Kesi ya kila mtu itachunguzwa katika mahakama ya mbinguni ( Warumi 14:10-12 ), na Mungu ataheshimu uchaguzi wa kila mtu kumtumikia Kristo au Shetani ( Ufunuo 22:11 , 12 ). Hatimaye, baada ya kuondoa dhambi, mpango wa Mungu ni kuumba mbingu mpya na dunia mpya ( 2 Petro 3:13 ; Isaya 65:17 ), ambapo dhambi haitatokea tena ( Nahumu 1:9 ), na kisha kuwapa watu Wake kama makao yao milele ( Ufunuo 21:1-5 ). Kisha Baba na Mwana watakaa pamoja na watu wao katika furaha kamilifu na upatanifu  wa milele.

Yote hii imejumuishwa katika "at-one-ment." Mungu ametujulisha hilo katika Neno Lake na kulidhihirisha katika ibada za Patakatifu pa Agano la Kale, haswa siku ya upatanisho. Yesu Ndiye ufunguo wa upatanisho. **Dhabihu Yake ya upendo kwa ajili yetu pale Kalvari inafanya yote yawezekane**. Kuondoa dhambi katika maisha yetu na katika ulimwengu kunawezekana kupitia **Yeye tu** ( Matendo 4:12 ). Si ajabu kwamba ujumbe wa mwisho wa sehemu/mambo matatu wa mbinguni kwa ulimwengu unatuita sisi sote kumwabudu Yeye ( Ufunuo 14:6 , 7 ).
Kwa nini mtu yeyote basi aondoe sehemu muhimu ya unabii huu?

**14. Kwa nini baadhi ya wafasiri wa Biblia wanatenga wiki ya mwisho (au miaka saba) ya miaka 490 iliyogawiwa taifa la Kiyahudi na kuitumia kwa kazi ya Mpinga Kristo mwishoni mwa historia ya ulimwengu?**

**Jibu:** Swali hili ni zuri "Kwa nini mtu yeyote aondoe miaka saba ya mwisho ya miaka 490 iliyotengewa taifa la Kiyahudi na kuiweka mwisho wa historia ya ulimwengu?"

**Hebu tupitie Ukweli**:
A. Hakuna **kibali**  au ushahidi wowote wa kuingiza pengo popote kati ya miaka yoyote ya unabii wa miaka 490. Kwani ni endelevu, yaani inaendelea, kama ilivyokuwa miaka 70 ya uhamisho wa watu wa Mungu iliyotajwa katika Danieli 9: 2 .

B. Kamwe katika Maandiko hakuna idadi maalum ya wakati uliotenga aidha (siku, wiki, miezi, miaka) inayojumuisha sehemu ya muda haimaanishi chochote isipokuwa vitengo vya wakati endelevu au mfululizo. Mzigo wa uthibitisho ni juu ya wale wanaodai kwamba sehemu yoyote ya wakati wowote unabii inapaswa kutengwa na kuhesabiwa baadaye.

C 27BK (mwaka wa ubatizo wa Yesu) ilikuwa tarehe ya kuanza kwa miaka saba ya mwisho ya unabii, ambayo Yesu alisisitiza kwa kuanza mara moja kuhubiri, "Wakati umetimia." Marko 1:15 .

D. Wakati wa kifo Chake msalabani katika majira ya kuchipua ya mwaka wa 31 BK, Yesu alipaza sauti, "Imekwisha." Mwokozi hapa anarejelea kwa uwazi unabii/ utabiri wa kifo Chake uliofanywa katika Danieli sura ya 9, kama vile:

1. "Masihi" "atakatiliwa mbali" au kusulubiwa (mstari wa 26).

2. "Angeikomesha dhabihu na dhabihu" kwa kufa kwa ajili ya wote kama Mwana-Kondoo wa kweli wa Mungu (mstari wa 27 1 Wakorintho 5:7). 15:3 ).

3. "Atafanya upatanisho kwa ajili ya uovu" (mstari 24).

Hakuna mamlaka ya kibiblia au ushahidi wa kutenganisha wiki ya mwisho, au miaka saba, ya miaka 490 iliyotengwa kwa taifa la Kiyahudi na kuitumia kwa kazi ya Mpinga Kristo karibu na mwisho wa historia ya ulimwengu. Kubwa zaidi, kutenganisha miaka saba iliyopita kutoka kwa unabii wa miaka 490 kwa namna hivyo kunapotosha maana ya Kweli ya unabii mwingi katika vitabu vya Danieli na Ufunuo hivi kwamba watu hawawezi kuuelewa kwa usahihi. Hii ndiyo sababu Mungu analaani tafsiri ya kibinafsi za unabii, kama vile nadharia hii ya pengo la miaka saba. Tafsiri kama hizo huwa zinawapotosha watu.

**15. Nimekubali dhabihu ya upatanisho ya Kristo kwa ajili ya maisha yangu na nimemwalika anitakase kutoka kwa dhambi na kunifanya mtu mpya.**

**Jibu:**
**Maswali ya mambo ya kucheua**
**1. Nguvu ya pembe ndogo inaonekana katika Danieli sura ya 7 na Danieli sura ya 8. Je, hizi zina nguvu sawa?**
Nguvu ya pembe ndogo ya Danieli 7 inaashiria upapa.
Nguvu ya pembe ndogo ya Danieli 8 inaashiria Rumi ya kipagani na ya kipapa.

**2. "Siku elfu mbili na mia tatu" ya Danieli 8:14 iliyotafsiriwa kihalisi kutoka kwa Kiebrania inasomeka "jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu". Je, hii inamaanisha siku 1,150, kama wengine wanavyobishana?**

La, Biblia huonyesha waziwazi katika Mwanzo 1:5 , 8 , 13 , 19 , 23 , 31 kwamba jioni na asubuhi ni sawa na siku moja. Hakukuwa na tukio lolote katika historia mwishoni mwa siku 1,150 ambalo lingetimiza unabii huu.

**3. Je, "uchaguzi" una sehemu gani katika maisha ya Mkristo?**
Ni ufunguo mkubwa wa mafanikio. Njia ya Mungu daima imekuwa na uhuru wa kuchagua ambayo inakufanya usilazimishwe kufanya jambo ila inakufanya ukomae na uwe na mawazo yako mwenyewe katika kumchagua Mungu au Shetani, na hivyo ukipewa uchaguzi, utampenda Mungu kiukwel na kwa moyo wako wote. ( Yoshua 24:15 ). Ingawa Mungu anataka kuokoa kila mtu ( 1 Timotheo 2:3 , 4 ), bado anaruhusu uchaguzi ufanyike kwa uhuru (Kumbukumbu la Torati 30:19 ). Mungu alimruhusu Shetani kuchagua kumwasi. Pia aliwaruhusu Adamu na Hawa wachague kutotii. Haki kamwe kufungiwa ndani, na kuwa kama kitu kilichopangwa

tayari ili kunipeleka mimi mbinguni bila ya kujali jinsi ninavyoishi au hata kama sitaki kwenda. Chaguo au kuchagua inamaanisha kuwa siku zote mimi niko huru kubadilisha mawazo yangu. Yesu ananiuliza nimchague Yeye ( Mathayo 11:28-30 ) na kuthibitisha chaguo langu kila siku ( Zaburi 86:3 ). Ikiwa chaguo langu la kila siku ni Kwake, atanibadilisha na kunifanya kama Yeye na hatimaye kunipeleka katika ufalme Wake mpya uliobarikiwa. Lakini tafadhali kumbuka, uko niko huru kugeuka na kwenda upande mwingine wakati wowote unaotaka au unaochagua. Mungu hatanilazimisha mimi au wewe kufanya kile tusichokipenda. Chaguo langu la kila siku la kumtumikia Yeye ni muhimu sana.

**4. Wengi wanaamini kwamba mfalme wa Seleucid Antioko Epifane ndiye mamlaka ya pembe ndogo ya Danieli 8. Je, tunawezaje kuwa na hakika kwamba hii si kweli?**

Kuna sababu nyingi. Baadhi yao ni kama ifuatavyo:
A. Antiochus Epiphanes hakuwa “mkuu kupita kiasi”, kama unabii unavyoamuru ( Danieli 8:9 ).

B. Hakutawala katika “wakati wa mwisho” au karibu na mwisho wa ufalme wa Seleucid kama unabii unavyotaja ( Danieli 8:23 ) lakini, badala yake, karibu na katikati.

C. Wale wanaofundisha kwamba Antiochus Epiphanes ndiye pembe ndogo huhesabu siku 2,300 kama siku halisi badala ya siku za kinabii sawa na mwaka. Kipindi hiki cha wakati halisi cha zaidi ya miaka sita hakina matumizi yenye maana kwa Danieli sura ya 8. Jitihada zote za kufanya kipindi hiki halisi cha wakati kilingane na Antioko Epifania zimeshindwa kwa namna moja, jambo ambalo limeleta aibu kwa wafuasi wake.

D. Pembe ndogo ingali ipo kwenye “wakati wa mwisho” ( Danieli 8:12 , 17 , 19 ), huku Antiochus Epiphanes alikufa mwaka wa 164 KK

E. Pembe hiyo ndogo ilipaswa kuwa “kuu kupita kiasi” upande wa kusini, mashariki, na Palestina ( Danieli 8:9 ). Ingawa Antiochus Epiphanes alitawala Palestina kwa muda, hakuwa na mafanikio yoyote huko Misri (kusini) na Makedonia (mashariki).

F. Pembe ndogo inatupa chini mahali pa Patakatifu pa Mungu ( Danieli 8:11 ). Antioko Epiphanes hakuharibu hekalu la Yerusalemu. Alilitia unajisi, lakini liliharibiwa na Warumi katika mwaka wa 70 BK. Wala hakuharibu Yerusalemu, kama ilisemwa na unabii ( Danieli 9:26 ).

G. Kristo alitumia machukizo ya uharibifu ya Danieli 9:26 na 27 , si kwa hasira za wakati uliopita za Antioko Epifania kRIK mwaka wa 167 KK, bali kwa wakati ujao wa karibu wakati jeshi la Kirumi lingeharibu Yerusalemu na hekalu katika kizazi chake katika mwaka wa 70 BK. ( Luka 21:20-24 ). Katika Mathayo 24:15 , Yesu alimtaja nabii Danieli kihususani kwa kusema kwamba utabiri wake wa Danieli 9:26 , 27 ungetimizwa wakati Wakristo wangeona (wakati ujao) chukizo la

uharibifu 'limesimama katika Patakatifu' katika Yerusalemu. Hii ni wazi kwamba watu wanaosema hivi hawakuelewa au wanataka mkanganyiko.

H. Yesu alihusisha kwa uwazi uharibifu wa Yerusalemu na kukataa kwa mwisho kwa Israeli kumkubali kama Mfalme na Mwokozi ( Mathayo 21:33-43 ) 23:37 , 38 Luka 19:41-44 ). Uhusiano huu kati ya kumkataa Masihi na uharibifu wa jiji na hekalu ndio ujumbe muhimu wa Danieli 9:26 , 27 . Ni ujumbe unaotangaza matokeo ya kuendelea kwa Israeli kumkataa Masihi - hata baada ya kupewa miaka 490 ya ziada ya majaribio ya upendo. Kutumia unabii huo kwa Antiochus Epiphanes, aliyekufa mwaka wa 164 KK, muda mrefu kabla ya kuzaliwa kwa Yesu, kunaharibu kabisa maana ya Danieli sura ya 8 na 9 - unabii wa wakati muhimu zaidi wa Biblia.

**Maswali ya Chemsha Bongo**

**1. Kondoo mume wa Danieli 8 anaashiria (1)**
_____ Babeli.
_____ Umedi-Uajemi.
_____ Ugiriki.
_____ Roma.

**2. Mbuzi-dume wa Danieli 8 anawakilisha nini? (1)**
_____ Misri.
_____ Palestina.
_____ Ugiriki.
_____ Ashuru.

**3. Nguvu ya pembe ndogo ya Danieli 8 inawakilisha (1)**
_____ Antiochus Epifane.
_____ Rumi, katika awamu zake za kipagani na kipapa.
_____ Kutoamini Mungu.
_____ Iraki.

**4. Siku ya upatanisho katika Israeli la kale ilikuwa siku ya hukumu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**5. Ni kiasi gani kati ya miaka 2,300 iliyokatiliwa mbali kwa ajili ya Wayahudi? (1)**
_____ miaka 490.
_____ miaka 700.
_____ miaka 1810.
_____ miaka 100.

**6. Katika unabii wa Biblia, siku moja ya unabii ni sawa na mwaka mmoja halisi. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**7. Unabii wa miaka 2,300 ulitabiriwa (miaka 500 kabla haujatukia) kwamba Masihi angetokea mwaka wa 27 BK. Alionekana kwa wakati ufaao. Hii inathibitisha kwamba (3)**
_____ Biblia imevuviwa.
_____ Malaika Gabrieli alikisia kwa bahati.
_____ Tarehe zingine zote katika unabii ni sahihi.
_____ Yesu Ndiye Masihi.

**8. Wakati miaka 490 iliyogawiwa taifa la Wayahudi ilipokwisha mwaka wa 34 BK, wanafunzi walifanya nini? (1)**
_____ Walianza kuwahubiria watu wa mataifa mengine.
_____ Walichukua likizo ndefu.
_____ Walisema kwamba hakuna Myahudi ambaye angeokolewa baada ya AD 34.

**9. Kulingana na unabii wa miaka 2,300 wa Danieli sura ya 8 na 9 , ni nini kilichotukia mwaka wa 1844? (1)**
_____ Hukumu ilianza mbinguni.
_____ Siku ya rehema kwa taifa la Kiyahudi iliisha.
_____ Yesu alipaa mbinguni.
_____ Mungu alifunga rehema kwa watu wote.

**10. Siku ya mbinguni ya upatanisho, au upatanisho mmoja, italeta ulimwengu wote katika mapatano kamili na Mungu. Ni kauli gani kati ya zifuatazo zinazosema Ukweli kuhusu sehemu fulani ya upatanisho? (10)**
_____ Yesu alitoa maisha Yake ili kulipa adhabu yetu ya kifo.
_____ Yesu alituweka huru kutoka katika hatia ya dhambi.
_____ Yesu anatubadilisha na kutufanya kuwa watu wapya kabisa.
_____ Yesu anaturudisha kwa mfano wa Mungu.
_____ Katika mahakama ya mbinguni, Mungu huheshimu chaguo la kila mtu kumtumikia Kristo au Shetani.
_____ Taarifa kamili huenda kwa kila mtu duniani kuhusiana na mpango wa Shetani wa kuharibu na mpango mtukufu wa Mungu wa kuwaokoa watu.
_____ Dhambi, Shetani, na wenye dhambi watatengwa na kuangamizwa.
_____ Mungu anaumba mbingu mpya na nchi mpya kwa ajili ya watu Wake na atakaa pamoja nao.
_____ Dhambi hainuka tena.
_____ Upatanisho uliwezekana kwa dhabihu ya Yesu pale Kalvari.
_____ Shetani na malaika zake wataongoka na kuokolewa.

**11. Hakuna mamlaka ya Biblia au ushahidi wa kutenganisha juma la mwisho au miaka saba ya miaka 490 iliyogawiwa taifa la Kiyahudi na kuitumia kwa kazi ya Mpinga Kristo karibu na mwisho wa historia ya ulimwengu. (1)**
_____ Kweli.
_____ Uongo.

**12. Mnamo mwaka wa 34 BK, (3)**
_____ Rehema iliisha kwa Wayahudi kama taifa teule la Mungu.
_____ Wanafunzi walianza kuwahubiria watu na mataifa mengine.
_____ Stefano, shemasi mwadilifu, alipigwa mawe.
_____ Hukumu ilianza mbinguni.

**13. Muda wa siku 2,300 ulianza katika (1)**
_____ BK 34
_____ 1944
_____ 1491 KK
_____ 457 KK

**14. Unabii wa Danieli na Ufunuo unatuhusu hasa sisi na wakati wetu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**Kesi Imefungwa**

**Somo la 19**

Mahakama inaendelea, hukumu imesomwa ... kesi imefungwa! Mawazo machache yanaweza kuwa ya kutisha zaidi ya haya Siku inakaribia upesi ambapo kila mtu ambaye amewahi kuishi, maisha yake yatapitishwa upya mbele ya macho ya Mungu yanayojua mambo yote ( 2 Wakorintho 5:10 ). Lakini usiruhusu hali hii ikupe mshtuko - jipe moyo! Mamilioni tayari wamepata ujumbe wa hukumu katika Mwongozo huu wa Mafunzo kuwa habari njema sana! Katika vipindi vinne ambapo kitabu cha Ufunuo kinataja hukumu kuu, sifa na shukrani inatokeza! Lakini je, unajua kwamba Biblia hutaja hukumu zaidi ya mara elfu moja? Karibu kila mwandikaji wa Biblia anarejelea hukumu, kwa hiyo umuhimu wake hausisitizwi kupita kiasi, maana upo kila mahali. Katika dakika chache zijazo, utapata ufafanuzi halisi katika somo hili lililopuuzwa.

Awamu ya Kwanza ya Hukumu ya Mwisho

**1. Malaika Gabrieli alimpa Danieli unabii wa hukumu ya mbinguni ya mwaka 1844. Awamu ya kwanza ya hukumu inaitwa hukumu kabla ya kuja kwa Yesu kwa sababu inafanyika kabla ya kuja kwa Yesu mara ya pili. Ni kundi gani la watu litakalozingatiwa katika awamu ya kwanza ya hukumu? Je, inaisha lini?**
“Hukumu lazima ianzie katika nyumba ya Mungu.” 1 Petro 4:17 . “Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu, na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki, na mtakatifu na azidi kutakaswa. tazama, Naja upesi, na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.” Ufunuo 22:11 , 12 . (Ona pia 1 Timotheo 3:15 .)

**Jibu: Hukumu i**naisha kabla tu ya ujio wa pili wa Yesu. Wale (walio hai na waliokufa)

waliodai kuwa Wakristo--"nyumba ya Mungu"--watapitiwa na hukumu ya kabla ya kuja kwa Yesu au kabla ya wale wasioamini. (Tarehe ya 1844 imeanzishwa katika Mwongozo wa 18.)

Yesu anasimama pamoja na watu Wake waaminifu katika hukumu na kuwaahidi uamuzi chanya.

**2. Ni nani anayesimamia hukumu? Wakili wa utetezi ni nani? Hakimu? Mshitaki? Mashahidi ni akina nani?**

"Mzee wa siku aliketi, ... kiti Chake cha enzi kilikuwa kama mwali wa moto." "Hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunguliwa." Danieli 7:9 , 10 . "Tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki." 1 Yohana 2:1 . "Baba ... amekabidhi hukumu yote kwa Mwana." Yohana 5:22 . "Ibilisi, ... ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu mchana na usiku." Ufunuo 12:9 , 10 . "Haya ndiyo anenayo Yeye aliye Amina, shahidi mwaminifu na wa Kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu." Ufunuo 3:14 . (Ona pia Wakolosai 1:12-15 .)

**Jibu:** Mungu Baba, Mzee wa siku, anaongoza katika hukumu. Naye Anakupenda sana ( Yohana 16:27 ). Shetani ndiye mshitaki wako pekee. Katika mahakama ya mbinguni, Yesu, ambaye anakupenda, rafiki yako mkubwa atakuwa wakili wako, hakimu, na shahidi wako. Naye anaahidi kwamba hukumu "itatolewa kwa ajili ya watakatifu. Au watakatifu watapewa hukumu" Danieli 7:22 , NEB.

Ushahidi unaotolewa katika hukumu unatoka katika vitabu vya mbinguni.

**3. Ni nini chanzo cha ushahidi uliotumika katika hukumu ya kabla ya majilio ya Bwana? Je, wote watahukumiwa kwa kiwango gani? Kwa kuwa Mungu tayari anajua kila kitu kuhusu kila mtu, kwa nini awe/pawe na hukumu?**

"Hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunguliwa." Danieli 7:10 . "Wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao." Ufunuo 20:12 . "Wao ... watahukumiwa kwa sheria ya uhuru." Yakobo 2:12 . "Tumefanywa kuwa tamasha kwa ulimwengu, na kwa malaika, na kwa wanadamu." 1 Wakorintho 4:9 .

**Jibu:** Ushahidi wa mahakama unatokana na vitabu ambavyo maelezo yote ya maisha ya mtu yameandikwa. Kwa waaminifu, kumbukumbu ya sala, toba, na msamaha wa dhambi itakuwa pale kwa wote kuona kama ushahidi hivi. Rekodi zitathibitisha kwamba nguvu za Mungu huwawezesha Wakristo kuishi maisha yaliyobadilika. Mungu anapendezwa na watakatifu Wake Naye atafurahia kushiriki ushahidi wa maisha yao. Hukumu itathibitisha kwamba hakuna "kuhukumiwa kwa wale walio katika Kristo Yesu, ambao hawaenendi kwa kufuata mwili, bali kwa Roho." Warumi 8:1 .

Sheria ya Amri Kumi ni kiwango cha Mungu katika hukumu ( Yakobo 2:10-12 ). Kuvunja sheria Yake ni dhambi ( 1 Yohana 3:4 ). Haki ya sheria itatimizwa na Yesu kwa watu Wake wote ( Warumi 8:3 , 4 ). Kudai kwamba hili haliwezekani ni kutilia shaka Neno la Yesu na nguvu zake.

Hukumu sio kumjulisha Mungu. Tayari Yeye ana habari kamili ( 2 Timotheo

2:19 ). Hata hivyo, watu waliokombolewa watakuwa wakija mbinguni kutoka katika ulimwengu ambao umeshushwa hadhi na dhambi. Malaika na wakaaji wa malimwengu mengine ambayo hayajaanguka bila shaka wangehisi wasiwasi kuhusu kumkaribisha mtu yeyote kwenye ufalme wa mbinguni, ufalme ule wa Mungu, mtu ambaye angeweza kuanzisha dhambi tena. Hivyo, hukumu itawafungulia kila undani wa mambo kinagaubaga na kujibu kila swali. Kusudi la kweli la Shetani sikuzote limekuwa kumdharau Mungu kuwa si Mwenye haki, mkatili, asiye na upendo, na asiye wakweli. Hii inafanya kuwa muhimu zaidi kwa viumbe vyote katika ulimwengu kujionea wenyewe jinsi ambavyo Mungu amekuwa na subira sana kwa wenye dhambi. Kuthibitishwa kwa tabia ya Mungu wetu, ndilo kusudi kuu la hukumu ( Ufunuo 11:16-19). 15:2-4 16:5 , 7 19:1 , 2 Danieli 4:36 , 37 ). Kumbuka kwamba sifa na utukufu hutolewa kwa Mungu kwa jinsi anavyoshughulikia hukumu.
Kila sehemu ya maisha ya mtu itapitiwa upya katika hukumu.

**4. Ni sehemu gani ya maisha ya mtu inazingatiwa katika hukumu ya kabla ya kuja Kwake? Nini kitathibitishwa? Zawadi zitaamuliwaje?**
"Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya." Mhubiri 12:14 . "Acheni [ngano na magugu] zikue pamoja mpaka wakati wa mavuno." "Mwana wa Adamu atawatuma malaika Zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme Wake machukizo yote.

Mathayo 13:30 , 41 . "Tazama, Naja upesi na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo." Ufunuo 22:12.

**Jibu:** Kila undani wa maisha utapitiwa upya, ikijumuisha mawazo na matendo ya siri. Kwa sababu hii, awamu hii ya kwanza ya hukumu pia inaitwa hukumu ya uchunguzi au hukumu ya upelelezi. Hukumu itathibitisha nani ataokolewa kati ya wale waliodai kuwa Wakristo. Bila shaka pia itathibitisha wale waliopotea, ambao majina yao hayakuhukumiwa katika hukumu ya kabla ya kuja Kwake. Ingawa tumeokolewa kwa neema, thawabu zitatolewa kulingana na kazi, matendo, au mwenendo, jambo ambalo linathibitisha ukweli wa imani ya Mkristo ( Yakobo 2:26).
Awamu ya Pili ya Hukumu ya Mwisho

**5. Ni kikundi gani kinachohusika katika hukumu ya mbinguni wakati wa miaka 1,000 ya Ufunuo sura ya 20? Je, ni nini madhumuni ya awamu hii ya pili ya hukumu?**

"Hamjui ya kuwa watakatifu watauhukumu ulimwengu?... Hamjui ya kuwa tutawahukumu malaika?"

1 Wakorintho 6:2 , 3 . "Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu." Ufunuo 20:4 .

**Jibu:** "Watakatifu," au watu wenye haki wa nyakati zote ambao Kristo anawachukua kwenda mbinguni katika wingu wakati wa kuja Kwake mara ya pili, watashiriki katika awamu hii ya pili ya hukumu.
Tuseme familia fulani imegundua kwamba mwana wao kipenzi aliyeuawa hakuwa

mbinguni. Lakini muuaji wakamwona huko mbinguni. Bila shaka wangehitaji majibu fulani. Awamu hii ya pili ya hukumu itajibu maswali yote ya wenye haki. Uhai wa kila mtu aliyepotea (aliyemo ndani ya orodha ya Shetani na malaika zake) utachunguzwa kwa uangalifu na wenye haki, ambao watakubaliana kabisa na maamuzi ya Yesu kuhusu thawabu kwa kila mmoja (Jury duty-Jopo la shahidi au wahakiki wa haki). Itakuwa dhahiri kwa wote kwamba hukumu si jambo la kiholela. Badala yake, itathibitisha tu uchaguzi ambao watu wamefanya tayari kumtumikia Yesu au bwana mwingine ( Ufunuo 22:11 , 12 ). (Kwa mapitio ya miaka 1,000, ona Mwongozo wa 12.)

Awamu ya Tatu ya Hukumu ya Mwisho

**6. Awamu ya tatu ya hukumu ya mwisho itafanyika lini na wapi? Ni kundi gani jipya litakalokuwepo katika awamu hii ya hukumu?**
"Miguu Yake itasimama siku hiyo juu ya mlima wa Mizeituni, ulio mbele ya Yerusalemu." "Na Bwana, Mungu wangu, atakuja, na watakatifu wote pamoja nawe." "Nchi yote itageuzwa kama nchi tambarare kutoka Geba mpaka Rimoni kusini mwa Yerusalemu. Zekaria 14:4 , 5 , 10 . "Nami mimi Yohana nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu mbinguni." Ufunuo 21:2 . "Na hiyo miaka elfu itakapotimia, Shetani ... atatoka kwenda kuwadanganya mataifa ... kuwakusanya pamoja kwa vita." Ufunuo 20:7 , 8 .
Waovu watajaribu kuushambulia mji mtakatifu.

**Jibu:** Awamu ya tatu ya hukumu itafanyika duniani mwishoni mwa miaka 1,000 ya Ufunuo sura ya 20, baada ya Yesu kurudi duniani pamoja na mji mtakatifu. Waovu wote ambao wamewahi kuishi, akiwemo Ibilisi na malaika zake, watakuwepo. Mwishoni mwa miaka 1,000, waovu waliokufa wa nyakati zote watafufuliwa ( Ufunuo 20:5 ). Shetani mara moja anaanzisha kampeni yenye nguvu ya propaganda ili kuwahadaa. Cha kushangaza, yeye afaulu kusadikisha mataifa ya dunia kwamba yanaweza kuliteka jiji takatifu.

**7. Nini kitatokea baadaye?**
"Wakapanda juu ya upana wa nchi, wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji ule uliopendwa." Ufunuo 20:9 .

**Jibu:** Waovu wanauzingira mji na kujiandaa kushambulia.
Awamu ya tatu ya hukumu itakatiza mpango wa kushambulia mji.
**8. Ni nini kinachokatiza mpango wao wa vita, na matokeo yatakuwa nini?**
"Nikawaona wafu, wadogo kwa wakubwa, wamesimama mbele za Mungu; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; sawasawa na kazi zao." Ufunuo 20:12 . "Lazima sisi sote tuonekane mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo." 2 Wakorintho 5:10 . "Kama Mimi niishivyo, asema Bwana, kila goti litapigwa mbele Zangu, na kila ulimi utakiri kwa Mungu. Hivyo basi, kila mmoja wetu atatoa hesabu yake mbele za Mungu." Waroma 14:11 , 12 .

**Jibu:** Bila kutarajia, bila onyo, Mungu anaonekana na mwangaza karibu wa kupooza juu ya jiji ( Ufunuo 19:11-21 ). Wakati wa Ukweli umefika. Kila nafsi

iliyopotea tangu ulimwengu ulipoanza, akiwemo Shetani na malaika zake, sasa inakabiliana kabisa na Mungu katika hukumu bila kuwa na shaka yoyote. Kila jicho limeelekezwa kwa Mfalme wa wafalme ( Ufunuo 20:12 ).

**Kila Mtu Huyaona Maisha Yake Mwenyewe Yakipitiwa**
Kisha kila nafsi iliyopotea inakumbuka visa au mambo yake mwenyewe ya maisha: Miito ya Mungu ya mara kwa mara, yenye uchangamfu, ya kusihi ili kutubu, ile sauti ya kushawishi, tulivu, ndogo usadikisho wa ajabu ambao mara nyingi ulikuja na mtu akakataa mara kwa mara kuitikia. Yote yapo. Usahihi wake hauwezi kupingwa. Ukweli wake haupingiki. Mungu anataka waovu waelewe kikamilifu.
Atatoa maelezo yoyote yanayotakikana ili kuweka mambo yote wazi. Vitabu na rekodi zinapatikana.

**Hakuna Kufunika**
Mungu hahusiki katika ufichaji fulani wa kimbingu. Hajaharibu ushahidi, hakufuta mkanda uliorekodi mambo! Hakuna cha kuficha. Kila kitu kiko wazi, na kila mtu ambaye amewahi kuishi pamoja na malaika wote wema na wabaya atakuwa akitazama drama hii kubwa kati ya drama zote (hautakuwa mchezo wa kuigiza bali matukio halisi).

**Kuanguka Kwenye Magoti kwa Waliopotea**
Ghafla kunatokea harakati. Nafsi moja iliyopotea inapiga magoti ili kukiri hatia yake na kukiri waziwazi kwamba Mungu alikuwa mwema na mwenye haki sana kwake. Kiburi chake na ukaidi kilimzuia kujibu sauti ya kusihi. Na kwenye pande zote sasa, watu na malaika waovu vile vile wanapiga magoti na kukiri. Kisha katika hatua moja kubwa, karibu wakati huo huo watu wote waliosalia na malaika waovu, pamoja na Shetani, wanaanguka kifudifudi mbele za Mungu ( Warumi 14:11 ). Wanalitoa hatia jina la Mungu kwa kulisafisha waziwazi kutokana na mashtaka yote ya uongo na kutoa ushahidi jinsi Yeye alivyowatendea kwa upendo, haki na rehema.

**Wote Wanakiri Kwamba Hukumu Ni Ya Haki**

Wote wanakiri kwamba hukumu ya kifo iliyotolewa juu yao ni ya haki njia pekee iliyo salama ya kushughulikia dhambi. Kwa kila mtu aliyepotea inaweza kusemwa, “Umejiangamiza mwenyewe.” Hosea 13:9 . Mungu sasa anasimama akiwa amethibitishwa mbele ya malimwengu yote. Mashtaka na madai ya Shetani yamefichuliwa na kukanushwa bila shaka kuwa ni uongo potovu wa mtenda dhambi mgumu.
Moto kutoka mbinguni utatuondoa dhambi na wenye dhambi milele

**9. Ni hatua gani za mwisho ambazo zitaondoa dhambi katika ulimwengu wote mzima na kuandaa makao salama na wakati ujao kwa waadilifu?**
“Wakaizunguka kambi ya watakatifu, ... na moto ukashuka kutoka kwa Mungu mbinguni, ukawala. Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika lile ziwa la moto.” Ufunuo 20:9 , 10 . “Kwa maana hao [waovu] watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu.” Malaki 4:3 . “Tazama, Mimi naumba mbingu mpya na

nchi mpya.” Isaya 65:17 . “Tazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake.” 2 Petro 3:13 . “Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, ... nao watakuwa watu Wake, na Mungu Mwenyewe atakuwa pamoja nao.” Ufunuo 21:3 .

**Jibu:** Moto kutoka mbinguni utawashukia waovu. Moto huo utaondoa kabisa dhambi na wenye dhambi kutoka kwa ulimwengu milele. (Ona Mwongozo wa 11 wa Masomo kwa habari kamili kuhusu moto wa mateso.) Huu utakuwa wakati wa huzuni na mshtuko mkubwa kwa watu wa Mungu. Karibu kila mtu atakuwa na mpendwa au rafiki kwenye moto. Malaika walinzi labda watatokwa na machozi kwa kupoteza watu waliowalinda na kuwapenda kwa miaka mingi. Hata Kristo bila shaka atawalilia wale aliowapenda na kuwasihi kwa muda mrefu sana. Wakati huo wa kutisha, uchungu wa Mungu, Baba yetu Mwenye upendo, juu ya gharama ya kutisha ya dhambi utakosa maelezo ya kibinadamu.

**Mbingu Mpya na Nchi**
Kisha Bwana atafuta machozi yote kutoka kwa watu Wake waliokombolewa ( Ufunuo 21:4 ) na kuumba mbingu mpya na dunia mpya yenye kupendeza kupita maelezo kwa watakatifu Wake. Na bora zaidi, Atakaa hapa pamoja na watu Wake katika milele zote. Hakuna mtu anayefikiri angetaka kukosa hilo.
Mnyama aliyetolewa dhabihu aliwakilisha dhabihu ya Yesu msalabani.

**10. Je, huduma ya “siku ya upatanisho” katika Patakatifu pa duniani ya Agano la Kale ilifananishaje hukumu na mpango wa Mungu wa kuondoa dhambi kutoka kwa ulimwengu na kurejesha mapatano kamilifu?**
**Jibu:** Katika Mwongozo wa 2 wa Somo, tulijifunza jinsi Shetani alivyomshtaki na kumpinga Mungu kwa uongo na kuleta uovu mbaya wa dhambi katika ulimwengu. Siku ya upatanisho katika Israeli ya kale ilifundisha, kwa njia ya mifano, jinsi Mungu atakavyoshughulikia tatizo la dhambi na kurudisha upatanisho kwa ulimwengu kwa upatanisho.
(Upatanisho unamaanisha “mapatano mamoja,” au “kuleta vitu vyote katika upatano kamili wa kimungu.”)

Katika Patakatifu pa duniani, hatua za mfano zilikuwa:

A. Mbuzi wa Bwana aliyechinjwa ili kufunika dhambi za watu.

B. Kuhani alinyunyiza damu mbele ya Kiti cha Rehema.

C. Hukumu ilifanyika kwa utaratibu huu:

(1) wenye haki walithibitisha, (2) wasiotubu kukatiliwa mbali, na (3) kumbukumbu ya dhambi kuondolewa katika Patakatifu.

D. Rekodi ya dhambi iliyowekwa juu ya mbuzi wa Azazeli.

E. Mbuzi wa Azazeli aliyetumwa nyikani.

F. Watu waliosafishwa na dhambi zao.

G. Wote wanaanza mwaka mpya kwa Ukrasa safi.

***<u>Hatua hizi tano za mfano zinawakilisha matukio halisi ya upatanisho ambayo yameanzishwa kutoka Patakatifu pa mbinguni,</u>*** makao makuu ya Mungu ya mbinguni kwa ulimwengu. Pointi ya kwanza hapo juu ni ishara ya tukio halisi la upatanisho wa pointi ya kwanza chini ya kipengele cha pointi y apili hapo juu ni ishara ya pointi ya pili hapa chini, n.k. Angalia jinsi Mungu anavyoonyesha kwa uwazi matukio haya makuu ya upatanisho:

A. Kifo cha dhabihu cha Yesu kama dhabihu badala ya mwanadamu ( 1 Wakorintho 15:3 5:7 ).

B. Yesu kama Kuhani wetu Mkuu anawarudisha watu kwa mfano wa Mungu ( Waebrania 4:14-16 Warumi 8:29 ).

C. Hukumu inatoa kumbukumbu kuthibitisha maisha, mema na mabaya, na kisha kuondoa kumbukumbu za dhambi kutoka Patakatifu pa mbinguni ( Ufunuo 20:12) Matendo 3:19-21 ).

D. Wajibu wa kuanzisha dhambi na kuwafanya watu wote watende dhambi umewekwa kwa Shetani ( 1 Yohana 3:8 ) Ufunuo 22:12 ).

E. Shetani alifukuzwa nyikani (miaka 1,000 ya Ufunuo sura ya 20).

F. Shetani, dhambi, na wenye dhambi wameondolewa kabisa ( Ufunuo 20:10 21:8 Zaburi 37:10 , 20 Nahumu 1:9 ).

G. Nchi mpya iliyojengwa kwa ajili ya watu wa Mungu. Kila kitu kilichopotea kwa dhambi kinarejeshwa kwa watakatifu wa Bwana ( 2 Petro 3:13 Matendo 3:20 , 21).

Upatanisho haujakamilika mpaka ulimwengu na vyote vilivyomo ndani yake virudishwe katika hali ya kabla ya dhambi kwa kuhakikisha kwamba dhambi hainuka tena.

Baada ya hukumu, dhambi itatoweka milele. Wenye haki watakuwa salama milele.

**11. Ni habari gani njema inayohusu hukumu ambayo imefunuliwa katika Mwongozo huu wa Somo na kuorodheshwa hapa chini?**
**Jibu:** A. Mungu na namna Yake ya kushughulikia tatizo la dhambi itathibitishwa kwa utukufu mbele ya ulimwengu mzima. Hili ndilo lengo kuu la hukumu.

B. Hukumu itaamuliwa kwa kuwapendelea watu wa Mungu.

C. Wenye haki watakuwa salama kutokana na dhambi milele.

D. Dhambi itaondolewa kabisa na haitatokea/haitaibuka mara ya pili tena.

E. Kila kitu ambacho Adamu na Hawa walipoteza kwa dhambi kitarejeshwa kwa waliokombolewa.

F. Waovu wataungua na kuwa majivu, na si kuteswa milele. Mungu hakuahidi uzima wa milele kwa waovu.

G. Katika hukumu, Yesu Ndiye hakimu, wakili, na shahidi wetu.

H. Baba na Mwana wote wanatupenda. Ibilisi ndiye anayetushtaki.

I. Vitabu vya mbinguni vitasaidia wenye haki kwa sababu vitaonyesha jinsi neema ya injili ilivyobadilisha maisha yao.

J. Hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Hukumu itadhihirisha Ukweli huo tu.

K. Hakuna nafsi hata moja (ya mtu au malaika) ambayo italalamika kwamba Mungu hana haki. Wote kwa pamoja wataona na kusema kwamba Mungu amekuwa na upendo, haki, neema, na fadhili katika kushughulika na wote.

**12. Mungu anaahidi kukuacha huru katika hukumu ya mbinguni ikiwa utamwalika aingie katika maisha yako na kumruhusu abaki kuwa mtawala wa maisha yako. Je, utamkaribisha kuingia katika maisha yako leo?**
**Jibu:**
**Maswali ya Kucheua**
**1. Kuna tofauti gani kati ya kumkubali Yesu kama Mwokozi wangu na kumkubali kuwa Bwana wangu?**

**Tofauti ni kubwa.**
Ninapomkubali kama Mwokozi, ananiokoa kutoka kwa hatia na adhabu ya dhambi na kunipa kuzaliwa upya. Ananibadilisha kutoka kuwa mwenye dhambi hadi kuwa mtakatifu. Shughuli hii ni muujiza wa utukufu na ni muhimu kwa wokovu. Hakuna anayeweza kuokolewa bila hilo. Hata hivyo, Yesu hajamalizana nami kwa wakati huu. Nimezaliwa, lakini mpango Wake ni kwamba mimi pia ninapaswa kukua na kuwa kama Yeye ( Waefeso 4:13 ). Ninapomkubali kila siku kama mtawala, au Bwana, wa maisha yangu, Yeye, kwa miujiza Yake, hunifanya nikue katika neema na mwenendo wa Kikristo hadi ninapokuwa mkomavu katika Kristo (2 Petro 3:18 ) .

**Shida - Nataka Njia Yangu Mwenyewe**
Tatizo ni kwamba nataka kuendesha maisha yangu - nataka kuwa na njia yangu mwenyewe. Biblia inaita hii "uovu", au dhambi ( Isaya 53:6). Kumfanya Yesu kuwa Bwana wangu ni muhimu sana hivi kwamba Agano Jipya linamtaja Yeye kama "**Bwana" mara 766. Katika kitabu cha Matendo pekee, anatajwa kama "Bwana" mara 110 na kama "Mwokozi" mara mbili tu. Hili linaonyesha jinsi ilivyo muhimu kumjua kama Bwana na Mtawala wa maisha yetu.**

**Sharti Lililopuuzwa - Kumfanya Bwana**

Yesu aliweka msisitizo unaoendelea juu ya Yeye kuwa Bwana kwa sababu Alijua kwamba kumvika taji ya Bwana kungekuwa jambo la kusahaulika na kupuuzwa ( 2 Wakorintho 4:5 ). NisipomfanyaYeye kuwa Bwana wa maisha yangu, basi hakuna njia ninayoweza kuwa Mkristo kamili aliyevikwa haki ya Kristo. Badala yake, nitaishia kuwa "mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi" na, mbaya zaidi, nitabaki kuhisi kwamba mimi niko sawa tu na "sihitaji chochote". Ufunuo 3:17 .

**2. Kwa kuwa kumbukumbu ya dhambi za watu wa Mungu ilihamishwa siku ya upatanisho kwa mbuzi wa Azazeli, je, hilo halimfanyi yeye pia kuwa mchukua-dhambi wetu? Nilifikiri Yesu pekee Ndiye aliyebeba dhambi zetu.**

Mbuzi wa Azazeli, ambaye anawakilisha Shetani, habebi kwa njia yoyote dhambi, au kulipia, dhambi zetu. Mbuzi wa Bwana, ambaye alitolewa dhabihu siku ya upatanisho, anawakilisha Yesu, aliyechukua na kulipia dhambi zetu pale Kalvari. Yesu peke yake "aichukuaye dhambi ya ulimwengu". Yohana 1:29 . Shetani ataadhibiwa (kama watenda dhambi wengine wote— Ufunuo 20:12-15 ) kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, ambazo zitajumuisha wajibu wa (1) uwepo wa dhambi zote, (2) matendo yake maovu, na (3) kuathiri kwake kila mtu. mtu duniani kufanya dhambi. Mungu atamwajibisha waziwazi kwa uovu. Hivi ndivyo ishara ya uhamisho wa dhambi kwa mbuzi wa Azazeli (Shetani) katika siku ya upatanisho inakusudia kuwasilisha.

**3. Biblia iko wazi kwamba Mungu husamehe dhambi zote zinazoungamwa (1 Yohana 1:9). Pia ni wazi kwamba, ingawa zimesamehewa, kumbukumbu za dhambi hizi zinabaki kwenye vitabu vya mbinguni hadi mwisho wa nyakati (Matendo 3:19-21). Kwa nini dhambi hazifutwi zikisamehewa?**

Kuna sababu nzuri sana. Hukumu ya mbinguni haitakuwa kamili hadi hukumu ya waovu itendeke— kabla tu ya maangamizo mwisho wa ulimwengu. Ikiwa Mungu angeharibu kumbukumbu kabla ya awamu hii ya mwisho ya hukumu, Angeweza kushutumiwa kwa ufichaji mkubwa wa kumbukumbu. Rekodi zote za maadili hubaki wazi ili kutazamwa, na kujionea wenyewe hadi hukumu itakapokamilika.

**4. Wengine wanasema hukumu ilifanyika pale msalabani. Wengine wanasema kwamba hufanyika wakati wa kifo. Je, tunaweza kuwa na uhakika wa muda wa hukumu kama inavyoonyeshwa katika Mwongozo huu wa Somo ni sahihi?**

Ndiyo. Ili kufanya iwezekane kwetu kuwa na uhakika kuhusu wakati wa hukumu, Mungu alitaja waziwazi mara tatu katika Danieli sura ya 7. Angalia wakati hususani wa Mungu. Mungu hakuacha nafasi ya kutokuwa na uhakika. Mfuatano wa Bwana umeelezwa mara tatu (mistari 8-14, 20-22, 24-27) katika sura hii moja kama ifuatavyo:

A. Nguvu ya pembe ndogo - ilitawala AD 538-1798. (Ona Mwongozo wa 15.)

B. Hukumu - inaanza baada ya 1798 (mwaka 1844) na inaendelea hadi ujio wa pili wa Yesu.

C. Ufalme mpya wa Mungu - ulioanzishwa mwishoni mwa hukumu.

Kwa hiyo Mungu anaweka wazi kwamba hukumu haifanyiki wakati wa kifo cha Yesu au msalabani, bali kati ya 1798 na ujio wa pili wa Yesu. Kumbuka kwamba ujumbe wa malaika wa kwanza ni sehemu yake, "Saa ya hukumu Yake imekuja". Ufunuo 14:6 , 7 . Watu wa Mungu wa nyakati za mwisho lazima wawe wanauambia ulimwengu kwamba hukumu ya mwisho inaendelea sasa!

**5. Tunaweza kujifunza mambo gani muhimu kutokana na funzo letu la hukumu?**

**Zingatia mambo matano yafuatayo:**

A. Mungu anaweza kuonekana kuchukua muda mrefu kabla ya kutenda, lakini wakati Wake ni sahihi. Hakuna mtu aliyepotea atakayeweza kusema "sikuelewa" au "sikujua".

B. Shetani na uovu wa kila aina hatimaye watashughulikiwa na Mungu katika hukumu. Kwa kuwa hukumu ni kazi ya Mungu Naye Ana Ukweli wote, tunapaswa kuacha kuwahukumu wengine na kumwacha Mungu aifanye Yeye Mwenyewe. Ni jambo zito kwetu kuchukua kazi ya Mungu ya kuhukumu. Ni kunyakua mamlaka Yake.

C. Mungu anatuacha sisi sote huru kuamua jinsi tutakavyohusiana Naye na ni nani tutakayemtumikia. Hata hivyo, ni lazima tuwe tayari kwa matokeo mabaya tunapoamua kinyume na Neno Lake.

D. Mungu anatupenda sana hata ametupa vitabu vya Danieli na Ufunuo ili kuyaweka wazi masuala haya ya nyakati za mwisho. Usalama wetu pekee upo katika kumsikiliza na kufuata ushauri wake kutoka katika vitabu hivi vikuu vya unabii.

E. Shetani amedhamiria kumwangamiza kila mmoja wetu. Mikakati yake ya udanganyifu ni yenye ufanisi na yenye kurubuni au kusadikisha watu hivi kwamba wote isipokuwa wachache sana watanaswa. Bila nguvu ya Yesu ya ufufuo katika maisha yetu kila siku ili kutulinda na mitego ya shetani, tutaangamizwa na Shetani.

**Maswali au Chemsha Bongo**

**1. Kuna awamu ngapi za hukumu? (1)**

_____ Sita.
_____ Moja.
_____ Tatu.

**2. Angalia vipengele vya kweli kuhusu awamu ya kwanza ya hukumu. (7)**

_____ Ni hukumu ya kabla ya majilio.
_____ Ilianza mwaka wa 1844.

_____ Inafanyika sasa.
______Shetani ndiye mshitaki.
_____ Malaika Gabrieli ndiye mwamuzi.
_____ Mungu anasimamia.
_____ Nabii Yona alitabiri.
_____ Sheria ya Mungu ndiyo kipimo.
_____ Atazingatia maisha ya wale waliodai kuwa Wakristo.

**3. Ni mambo gani yanayosema Ukweli kuhusu awamu ya pili ya hukumu, ambayo itafanyika wakati wa miaka 1,000? (3)**
_____ Wenye haki wa nyakati zote watakuwepo.
_____ Shetani ataendelea kukatiza shughuli za mahakama zinazoendelea.
_____ Wote watakubali kwamba adhabu ya Shetani ni ya haki.
_____ Malaika wa Shetani watasamehewa.
_____ Waovu watadai haki zao.
_____ Wenye haki watajifunza kwa nini baadhi ya marafiki zao wamepotea.

**4. Yesu atahudumu katika nyadhifa tatu. Wao ni kina nani? (3)**
_____ Jaji.
_____ Shahidi.
_____ Mdhamini.
_____ Karani wa mahakama.
_____ Wakili wa utetezi.

**5. Waovu watakuwepo kwa ajili ya hukumu mwishoni mwa miaka 1,000 baada ya kuuzunguka mji mtakatifu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**6. Mungu ataweka wazi kwa kila mtu aliyepotea na malaika kwa nini amepotea. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**7. Katika awamu moja ya hukumu kila mtu (wema na mbaya) ambaye amewahi kuishi, pamoja na malaika wote waovu na Shetani, atakuwepo ana kwa ana. Awamu gani? (1)**
_____ Awamu ya kwanza—hukumu ya sasa ya kabla ya kuja.
_____ Awamu ya pili—katika kipindi cha miaka 1,000.
_____ Awamu ya tatu—mwishoni mwa miaka 1,000.

**8. Kwa nini vitabu vya kumbukumbu vinahitajika katika hukumu ya mbinguni? (1)**
_____ Kumjulisha Mungu Ukweli.
_____ Kumkumbusha Mungu kile ambacho huenda amesahau.
_____ Kuwapa malaika kitu cha kufanya.
_____ Ili kuwasaidia watu, malaika, na wakaaji wa ulimwengu mwingine kuelewa

jinsi Mungu anavyoshughulikia hukumu bila upendeleo na kwa haki.

**9. "Upatanisho" maana yake ni "kuleta vitu vyote katika mapatano kamili na Mungu." Ni vitu gani hapa chini ni sehemu ya upatanisho mkuu wa mbinguni? (5)**
_____ Kifo cha Yesu msalabani.
_____ Hukumu.
_____ Huduma ya Yesu kama Kuhani wetu Mkuu.
_____ Gharika ya siku za Nuhu.
_____ Danieli katika tundu la simba.
_____ Uharibifu wa mwisho wa dhambi na wenye dhambi.
_____ Uumbaji wa mbingu mpya na nchi mpya.

**10. Ni mambo gani ambayo ni habari njema kutoka kwenye hukumu? (5)**
_____ Hukumu itaamuliwa kwa ajili ya watakatifu.
_____ Ibilisi ataungua moto milele kuzimu.
_____ Dhambi haitainuka tena.
_____ Dhambi inaweza kuanza tena kwa urahisi katika siku za usoni.
_____ Yesu Ndiye mwamuzi, wakili na shahidi wetu.
_____ Njia ya Mungu ya kushughulika na dhambi na wokovu itathibitishwa kikamilifu.
_____ Kila kitu ambacho Adamu na Hawa walipoteza kwa dhambi kitarejeshwa.

**11. Ukweli ni upi kuhusu Shetani kama mbuzi wa Azazeli wa hukumu? (3)**
_____ Anaadhibiwa kwa kuanzisha dhambi.
_____ Anaadhibiwa kwa kumwongoza kila mtu katika dhambi.
_____ Hana uhusiano wowote na kulipia dhambi zetu.
_______ Shetani atakataa kuwa mbuzi wa Azazeli na atatoroka.

**12. Hukumu si ya kiholela. Badala yake, inathibitisha kimsingi maamuzi ambayo watu tayari wamefanya ama kumtumikia Yesu au kuchagua bwana mwingine. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**13. Kusudi kuu la hukumu ni kuwafahamisha watu, Shetani, malaika wema na wabaya, na wakazi wa ulimwengu mwingine kwamba Mungu ameshughulikia janga la dhambi kwa hekima, kwa usawa, na kwa uadilifu tangu kuanza kwake huko mbinguni. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**Alama ya Mnyama**

**Maandiko: Ufunuo 13:1-8 , Ufunuo 14:9-18**

**Somo la 20**

Nambari ya tattoo, chip ya kompyuta chini ya ngozi, au kitu cha hila zaidi? Ni mojawapo ya unabii uliotafsiriwa vibaya sana katika Biblia yote - lakini ni muhimu sana kuelewa somo hili kwa usahihi. Lakini katika kusoma alama ya mnyama, ni lazima kushughulikia masuala nyeti sana, kutaja majina na kuwa mahususi. Hili si jambo linalopendwa na watu wengi leo, lakini ni lazima tuwe imara kwa sababu Mungu anawapenda watu Wake na anataka waijue Kweli. Ujumbe huu si kutoka kwetu sisi, bali ni wa Yesu. Na kifo cha milele kikiwakabili wale wanaopokea alama, itakuwa ni hatia kutomsaidia Yeye Bwana kutoa ujumbe huu Waamuzi 5:23. Somo hili pengine linapaswa kutanguliwa na onyo: "IBILISI HATAKI USOME NA KUKAMILISHA MWONGOZO HUU WA KUJIFUNZA." Tafadhali soma Ufunuo 13:1-8 , 14:9-12 , na 16-18 , na uombe Roho Mtakatifu akupe moyo mwaminifu na wenye kuelewa kabla ya kuanza safari hii ya kujifunza.

**Tujikumbushe kwa Haraka**

Tulijifunza kutoka kwa Mwongozo wa 2 kwamba Pambano la kutisha linaendelea kati ya Mungu na shetani. Limekuwa likiendelea kwa karne nyingi tangu Lusifa, malaika aliyekuwa na cheo kikubwa kati ya malaika wa mbinguni, akamwasi Mungu. Akiwa na malaika waliojiunga naye, alijaribu kumshinda Mungu na kutwaa udhibiti wa ulimwengu wetu. Mungu na malaika waaminifu hawakuwa na chaguzi nyingine ila kumfukuza Lusifa na malaika zake kutoka mbinguni. Lusifa, ambaye alikuja kujulikana kama Ibilisi na Shetani, alikasirika. Azimio lake la kumwangamiza Mungu na kudhibiti ulimwengu likaongezeka kila siku. Cha kushangaza, yeye ameungwa mkono na watu wengi zaidi duniani katika uasi wake. Bwana pia anaomba uaminifu na msaada wa watu, lakini Yeye huwaacha watu wawe huru kuchagua. Hivi karibuni kila mtu duniani atakuwa amejiunga na Shetani au Mungu. Vita vya mwisho kati ya Shetani na Mungu viko njiani, na vinaelezwa katika kitabu cha Ufunuo. Kitabu hiki kinaonyesha kwamba Mungu ana ishara, au alama, au uhuru ambao utawatambulisha watu Wake. Shetani pia ana alama, au ishara, ambayo itawatambulisha wale wanaomuunga mkono. Kama kawaida, Shetani atafanya kazi kupitia mamlaka ya kidunia iliyofananishwa na Ufunuo na mnyama ili kuweka alama yake. Mwongozo huu wa Somo utafunua alama ya mnyama, ambayo kila mtu aliyepotea wa wakati wa mwisho atapokea. Isipokuwa unajua nini maana ya "alama" yake ni nini, Je, wewe utawezaje kuepuka kuipokea?

**Upapa ni mpinga Kristo.**

**1. Ili kujua "alama" ni nini, ni lazima kwanza tutambue mnyama. Je, Biblia inamfafanuaje mnyama huyo?**

**Jibu:** Ufunuo 13:1-8 , 16-18 hutoa sifa 11 zinazowatambulisha. Yameorodheshwa

hapa chini:

A. Anainuka kutoka baharini (mstari wa 1).
B. Mkusanyiko wa wanyama wanne wa Danieli sura ya 7 (mstari wa 2).
C. Joka humpa nguvu na mamlaka (mstari wa 2).
D. Anapokea jeraha la mauti (mstari 3).
E. Jeraha la mauti linaponywa (mstari 3).
F. Nguvu kubwa ya kisiasa (mistari 3, 7).
G. Nguvu za kidini zenye nguvu (mistari 3, 8).
H. Dhambi ya kukufuru itahusika (mistari 1, 5, 6).
I. Atapigana na watakatifu na kuwashinda (mstari 7).
J. Atatawala kwa muda wa miezi 42 (mstari wa 5).
K. Ana namba ya ajabu 666 (mstari wa 18).

Je, baadhi ya pointi hizi zina vitabia vinavyojulikana? Hakika! Tulikutana na wengi wao hapo awali tulipojifunza kuhusu Mpinga Kristo katika Danieli sura ya 7. "Mnyama" wa Ufunuo 13 ni jina lingine la "Mpinga Kristo," ambalo tulijifunza kutoka kwa Danieli 7 ni upapa.

Unabii wa Danieli na Ufunuo mara nyingi hushughulikia msingi uleule wa unabii uliotangulia, lakini kila mara mambo mapya yanapoongezwa ambayo husaidia kufanya unabii huo kuwa hakika. Kwa hivyo tarajia kujifunza mambo mapya kuhusu Mpinga Kristo kutoka kwa Mwongozo huu wa Mafunzo. Sasa hebu tuzingatie, moja baada ya nyingine, pointi 11 zinazomwelezea mnyama.

A. Ingeinuka kutoka baharini ( Ufunuo 13:1 ).
Bahari (au maji) katika unabii inahusu watu, au eneo la watu ( Ufunuo 17:15 ). Kwa hiyo mnyama, au Mpinga Kristo, angetokea kati ya mataifa yenye nguvu na sauti katika ulimwengu uliojulikana wakati huo, na wa zamani yaani Ulaya, siyo mabara mapya kama vile Marekani au Australia. Upapa, kama tunavyojua sote, ulizuka Ulaya Magharibi, kwa hiyo unahusiana na jambo hili.

**Neno la Ufafanuzi**
Kwa Kupatana na amri ya Mungu ya kuwaheshimu watu wote ( 1 Petro 2:17 ), tunatulia hapa ili kutambua upapa kwa matendo yake ya huduma na utendaji wake mwingi mzuri katika mambo mengi. Hospitali zake, mashule yake ambayo yamewasaidia watu kwa elimu nchi nyingi, nyumba za watoto yatima, kulea maskini, nyumba za akina mama wasioolewa, wanasheria wake ambao wamewatetea wanyonge, matunzo ya wazee yanathaminiwa ulimwenguni pote nk. Wapendwa hawa wanaweza kusifiwa kwa uaminifu wa mambo mengi. Lakini, kama mashirika mengine yote, pia wamefanya makosa. Mungu anabainisha baadhi ya makosa yake katika Ufunuo. Bwana, ambaye hubariki na kufariji, lazima wakati mwingine anidhamishe na kusahihisha. Tafadhali mwombe Roho Wake azungumze nawe unapojifunza mada hii muhimu.

B. Huu ni mchanganyiko wa Wanyama wa Danieli sura ya 7 ( Ufunuo 13:2 ). Jifunze mlinganisho hapa chini ili kuona jinsi yote yanavyohusiana:

| | Danieli sura ya 7 | Ufunuo sura ya 13 |
|---|---|---|
| Babeli | Mnyama anayefanana na simba (mst. 4) | “Mdomo wa simba” (mst. 2) |
| Umedi na Uajemi | Mnyama kama dubu (mst. 5) | “Miguu ya dubu” (mst. 2) |
| Ugiriki | Mnyama anayefanana na Chui (mst. 6) | “Kama chui” (mst. 2) |
| Roma | Mnyama mwenye pembe kumi (mst. 7) | “Kuwa na ... pembe kumi” (mst. 1) |

Wanyama wanne wa Danieli 7 wanaonyeshwa kama sehemu ya Mpinga Kristo, au mnyama, kwa sababu upapa ulijumuisha imani na mazoea ya kipagani kutoka kwenye milki zote nne. Aliwavisha mavazi ya kiroho na kuyaeneza ulimwenguni kama mafundisho ya Kikristo. Hapa kuna mojawapo ya kauli nyingi za kuunga mkono kutoka kwa historia: “Kwa namna fulani, yeye [upapa] amenakili muundo wa shirika lake kutoka kwa Milki ya Kirumi, naye amehifadhi na kuzaa matunda yenye mawazo ya kifalsafa ya Socrates, Plato, na Aristotle, yaliyoazimwa kutoka Wenyeji wasiokuwa waungwana (barbarians) na wale waungwana wa Rumi wa himaya ya Byzantine, lakini daima anabaki kuwa yeye mwenyewe, akikusanya kikamilifu vitu vyote vilivyotolewa kutoka kwa vyanzo vya nje.” 1 Kipengele hiki kwa hakika kinaendana na upapa.

C. Mnyama lazima apokee uwezo wake, kiti chake (mji mkuu), na mamlaka yake kutoka kwa joka ( Ufunuo 13:2 ).
Ili kutambua joka, tunakwenda kwenye Ufunuo sura ya 12, ambapo kanisa la Mungu la wakati wa mwisho linaonyeshwa kama mwanamke safi. Katika unabii, mwanamke safi anawakilisha watu wa Kweli wa Mungu au kanisa ( Yeremia 6:2). Isaya 51:16 ). (Katika Mwongozo wa 23, tutawasilisha somo la kina la kanisa la Mungu la wakati wa mwisho la Ufunuo sura ya 12. Mwongozo wa 22 unafafanua Ufunuo sura ya 17 na 18, ambapo makanisa yaliyoanguka yanafananishwa na mama aliyeanguka na binti zake walioanguka.) Mwanamke anaonyeshwa kama mjamzito na karibu kujifungua. Joka hilo hujilaza karibu, likitumaini “kummeza” mtoto wakati wa kuzaliwa. Hata hivyo, mtoto anapozaliwa Yeye hukwepa Lijoka hilo, Naye hutimiza utume Wake, na kisha kupaa mbinguni. Kwa wazi Mtoto huyo ni Yesu, ambaye Herode alijaribu kumwangamiza kwa kuwaua watoto wote wachanga katika Bethlehemu ( Mathayo 2:16 ). Kwa hiyo joka hilo linawakilisha Rumi ya kipagani, ambayo Herode alikuwa mfalme wake. Nguvu nyuma ya njama ya Herode ilikuwa, bila shaka, shetani ( Ufunuo 12:7-9 ). Shetani hutenda kupitia serikali mbalimbali ili kukamilisha kazi yake mbaya katika kesi hii, alitumia Rumi ya kipagani.

Tutanukuu marejeo mawili tu ya kuunga mkono kutoka kwenye historia, ingawa yapo mengi: (1) “Kanisa la Kirumi ... lilijisukuma lenyewe hadi mahali pa Milki ya Ulimwengu ya Kirumi, ambayo ni mwendelezo wake halisi. ... Papa ... ndiye mrithi wa Kaisari.” 2 (2) “Kanisa la Kikatoliki lenye nguvu lilikuwa kidogo kama Dola ya Kirumi iliyobatizwa. Rumi ilibadilishwa na pia kuongoka. Mji uleule mkuu wa Dola ya kale ya kale ya Rumi, ukawa mji mkuu wa Dola ya Kikristo. Ofisi ya Pontifex

Maximus iliendelea kuwa ya Papa." 3 Kwa hiyo kipengele hiki pia kinaendana na upapa. Alipokea mji wake mkuu kutoka kwa mamlaka ya Rumi ya kipagani.

D. Angepokea jeraha la mauti ( Ufunuo 13:3 ).
Jeraha la mauti lilitolewa wakati jenerali wa Napoleon, Alexander Berthier alipoingia Roma na kumteka Papa Pius VI katika Februari 1798. Napoleon aliamuru kwamba wakati wa kifo cha papa, upapa ungekomeshwa. Papa alikufa huko Ufaransa mnamo Agosti 1799. "Nusu ya Ulaya ilifikiri ... kwamba bila Papa Upapa ulikuwa umekufa." 4 Hivyo kipengele hiki kinaendana na upapa (kimetimiza hii sifa).

E. Jeraha la mauti lingepona, na ulimwengu mzima
ngempa mnyama heshima/ungemwabudu ( Ufunuo 13:3 ).
Tangu kuponywa kwake kwa jeraha, nguvu ya shirika la upapa imekua na kuongezeka hadi leo yeye ni mojawapo ya mashirika yenye nguvu zaidi ya kidini-kisiasa na vituo vya ushawishi duniani. Malachi Martin, mtaalamu kamili wa mambo ya ndani wa Vatikani na mtaalamu wa akili, anafichua yafuatayo katika kitabu chake kinachouzika vyema, kiitwacho 'The Keys of This Blood' 5 (nambari za kurasa kwenye mabano):

**KUHUSU PAPA:**
Ameazimia kuwa mtawala wa ulimwengu kama vile Konstantino katika siku zake (49). Analindwa na serikali nne (120). Yeye ndiye mtu anayejulikana sana katika karne ya 20 (123). Yeye ni rafiki wa kibinafsi na viongozi wa nchi 91 (490). Watu wa ulimwengu wanaonekana kuwa tayari kwa serikali yake yenye maadili na kudhibiti ifanye kazi duniani yote (160). Waandishi wa habari elfu kumi na sita waliripoti ziara yake ya Marekani (490).

**KUHUSU UPAPA:**

Balozi wa Marekani anasema Vatikani haiwezi kulinganishwa na yoyote kama "Gazeti Linalosikilizwa" (120). Vatikani inajua fika kufikia Jumamosi kitakachotokea Jumatatu popote duniani (439). Muundo wa Papa umetayarishwa kutawala dunia nzima sasa (143).

Ni kweli isiyopingika kwamba jeraha limepona na macho ya mataifa yako juu ya Vatikani, kwa hiyo hatua hii pia inaendana na sifa ya upapa.

F. Ingekuwa mamlaka yenye nguvu kubwa ya kisiasa ( Ufunuo 13:3 , 7 ).
Tazama kipengele E hapo juu.

G. Lingekuwa shirika la kidini lenye nguvu sana ( Ufunuo 13:3 , 8 ).
Tazama kipengee E hapo juu.

H. Ingekuwa na hatia ya kukufuru ( Ufunuo 13:5 , 6 ).
Upapa una hatia ya kukufuru kwa sababu makasisi wake wanadai kusamehe dhambi na mapapa wake wanadai kuwa ndiye Kristo.

I. Ingepigana na kuwatesa watakatifu ( Ufunuo 13:7 ).

Upapa uliwatesa na kuwaangamiza mamilioni ya watakatifu wakati wa Nyakati za Giza (Inquistion).

J. Utawala huo ungetawala kwa muda wa miezi 42 ( Ufunuo 13:5 ).
Upapa ulitawala kwa muda wa miezi 42 ya kinabii, ambayo ni sawa na miaka 1,260, kuanzia mwaka 538-1798 BK.

Pointi H hadi J pia zinaendana na sifa za upapa. Tulizigusia kwa ufupi tu hapa kwa sababu zilishughulikiwa kwa kina katika Mwongozo wa Kusoma 15, swali la 8, vipengele E, G, na H.

K. Utawala huo Ungekuwa na nambari ya ajabu 666 ( Ufunuo 13:18 ). Mstari huu unasema, "Ni hesabu ya mwanadamu," na Ufunuo 15:2 inasema ni "hesabu ya jina lake." Je, unamfikiria mtu gani unapofikiria upapa? Kwa kawaida, sote tunamfikiria papa. Jina lake rasmi ni nani? Hapa kuna nukuu ya Kikatoliki: "Cheo cha papa wa Rumi ni "Vicarius Filii Dei" (Kiingereza: "Vicar of the Son of God").6 Malaki Martin, katika The Keys of This Blood, anatumia jina lile lile kwa ajili ya papa kwenye ukurasa wa 114, 122. Maelezo ya chini ya Ufunuo 13:18 katika matoleo fulani ya Biblia ya Douay [Katoliki] yanasema, "herufi zenye hesabu za jina lake ndizo zitafanyiza nambari hii."

Tena, upapa unapatana na sehemu ya utambulisho. mnyama mwenye "alama" ni upapa. Hakuna mamlaka nyingine katika historia ingeweza kupatana na mambo haya ya maelezo ya Bwana katika Neno Lake. Sasa kwa kuwa tumemtambulisha mnyama huyo kwa hakika, tunaweza kugundua alama yake, au ishara ya mamlaka. Lakini kwanza, hebu tuangalie Neno la Mungu. ishara ya mamlaka 1Andre Retif, The Catholic Spirit, trans. by Dom Aldhelm Dean, Vol. 88 of The Twentieth Century Encyclopedia of Catholicism (New York, Hawthorne Books, 1959), p. 85. 2Adolf Harnack, Ukristo ni nini na Thomas Bailey Saunders (New York: Putnam, toleo la 2, rev., 1901), uk. 270.

3Alexander Clarence Flick, The Rise of the Mediaeval Church (kuchapishwa tena: New York, Burt Franklin, 1959), uk. 148 , 149.

4Joseph Rickaby, "The Modern Papacy," Lectures on the History of Religion, Hotuba ya 24, (London: Catholic Truth Society, 1910), p. 1.

5(New York, Simon & Schuster, 1990)

6"Majibu kwa Maswali ya Wasomaji," Our Sunday Visitor, Nov. 15, 1914.
**Sabato ni ishara, au alama, ya nguvu za Mungu.**

**2. Alama ya Mungu au ishara ya mamlaka ni nini?**
"Naliwapa sabato Zangu ziwe ishara kati ya Mimi na wao, wapate kujua ya kuwa

Mimi, Bwana, Ndimi niwatakasaye." Ezekieli 20:12 . "Ni ishara kati ya Mimi na wana wa Israeli milele; maana kwa siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi." Kutoka 31:17 .

**Jibu:** Mungu anasema katika maandiko hapo juu kwamba alitupa Sabato Yake kama ishara tukufu ya uwezo Wake wa kuumba na uwezo Wake wa kututakasa (kugeuza na kuokoa) sisi. Katika Biblia, maneno muhuri, ishara, alama, na ishara yanatumiwa kwa kubadilishana.7 Ishara ya Mungu, Sabato, inawakilisha nguvu Zake takatifu za kutawala akiwa Muumba na Mwokozi. Ufunuo 7:1-3 inasema itaandikwa kwenye vipaji vya nyuso (akili, Waebrania 10:16 ) za watu Wake. Itaashiria kwamba wanamilikiwa Naye na wana tabia Yake. Waebrania 4:4-10 inathibitisha hili kwa kusema kwamba tunapoingia katika pumziko Lake (kupokea wokovu), tunapaswa kuitakasa Sabato Yake ya siku ya saba kama ishara, au alama, ya wokovu. Utunzaji Sabato wa Kweli humaanisha kwamba mtu amekabidhi maisha yake kwa Yesu Kristo na yuko tayari kufuata popote Yesu anapoongoza.

Kwa kuwa ishara, au alama, ya mamlaka na nguvu za Mungu ni siku Yake takatifu ya Sabato, inaonekana yaelekea kwamba ishara, au alama, ya mpinzani wa Mungu, mnyama, inaweza pia kuhusisha siku takatifu. Hebu tuone ikiwa inafanya.

7(Linganisha Mwanzo 17:11 na Warumi 4:11 na Ufunuo 7:3 na Ezekieli 9:4 .)

**Jumapili kama siku takatifu ni alama ya mnyama, au ishara ya mamlaka.**

**3. Upapa unasema nini ishara au alama yake ya mamlaka?**

**Jibu:** Angalia sehemu ifuatayo kutoka kwa katekisimu ya Kikatoliki:

**"Swali** : Je, una njia nyingine yoyote ya kuthibitisha kwamba Kanisa lina uwezo wa kuanzisha sherehe za kanuni?"

**"Jibu:** Kama Lisingekuwa na uwezo huo, basi Lisingeweza kufanya yale ambayo wanadini wote wa kisasa wanakubaliana naye -Lingeweza kuchukua nafasi ya utunzaji wa Jumapili kama siku ya kwanza ya juma, kwa kuadhimisha Jumamosi siku ya saba, mabadiliko ambayo hakuna mamlaka ya Kimaandiko." 8

Kwa hiyo upapa hapa unasema kwamba Ulibadilisha Sabato kuwa Jumapili na kwamba karibu makanisa yote yalikubali siku mpya takatifu kutoka kwao. Hivyo, upapa hudai kwamba Jumapili kuwa siku takatifu ndiyo alama, au ishara, ya uwezo na mamlaka yake.

8Stephen Keenan, A Doctrinal Catechism [FRS No. 7.], (3rd American ed., rev.: New York, Edward Dunigan & Bro., 1876), p. 174.

**Kubadilisha Sabato kuwa Jumapili kunahusisha kubadilisha sheria ya Mungu – jambo zito sana.**

**4. Je, Mungu alitabiri mabadiliko hayo katika Maandiko?**

**Jibu:** Ndiyo! Katika kueleza Mpinga Kristo katika Danieli 7:25 , Mungu alisema

itafikiri “kubadili majira na sheria.”

A. Upapa umejaribuje kubadili sheria za Mungu? Kwa njia tatu tofauti: Katika katekisimu zake (1) Umeacha amri ya pili dhidi ya kuabudu sanamu, na (2) kufupisha amri ya nne (Sabato) kutoka maneno 94 hadi nane tu. Amri ya Sabato (Kutoka 20:8-11 ) inabainisha wazi kuwa Sabato ni siku ya saba ya juma. Kama ilivyobadilishwa na upapa, amri inasomeka: “Kumbuka kwamba uitakase siku ya Sabato.” Imeandikwa hivyo, inaweza kurejelewa siku yoyote. Na, hatimaye, yeye (3) aligawanya amri ya kumi katika amri mbili.

B. Upapa umejaribuje kubadili nyakati za Mungu? Kwa njia mbili: (1) Amebadilisha wakati wa Sabato kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza. (2) Pia amebadilisha “muda” wa Mungu kwa ajili ya kuanza na kufunga saa za Sabato. Badala ya kuhesabu siku ya Sabato kuanzia machweo ya jua Ijumaa usiku hadi machweo ya jua Jumamosi usiku kama Mungu aagizavyo ( Mambo ya Walawi 23:32 ), alikubali desturi ya kipagani ya Warumi ya kuhesabu siku kuanzia saa sita usiku Jumamosi usiku hadi saa sita usiku Jumapili usiku. Mungu alitabiri “mabadiliko” haya yangedirikiwa au kufanyiwa utubuthu na mnyama, au Mpinga Kristo.

**Angalia sehemu ifuatayo kutoka kwa katekisimu ya Kikatoliki:**

“ **Swali:** Siku ya Sabato ni ipi?

**Jibu:** Jumamosi ni siku ya Sabato.

**Swali:** Kwa nini tunaadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi?

**Jibu:** Tunaadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu Kanisa Katoliki lilihamisha sherehe kutoka Jumamosi hadi Jumapili.” 9

Hapa kuna usemi mwingine wa Kikatoliki: “Kanisa liko juu ya Biblia na kuhamisha huku kwa siku ya utunzaji wa Sabato kutoka Jumamosi hadi Jumapili ni uthibitisho chanya wa ukweli huo.” 10

Upapa unasema katika rejeleo hizi kwamba mabadiliko yake yenye mafanikio ya utunzaji wa Sabato hadi ibada ya Jumapili ni uthibitisho kwamba mamlaka yake ni kuu zaidi, au “juu,” Maandiko.

9Peter Geiermann, The Convert’s Catechism of Catholic Doctrine (St. Louis, B. Herder Book Co., 1957 ed.), p. 50.

10Rekodi ya Kikatoliki (London, Ontario, Kanada, Septemba 1, 1923).
**Upapa umebadilisha Sabato kuwa Jumapili.**

**5. Mtu yeyote angewezaje kuthubutu kujaribu kubadili siku takatifu ya Mungu?**
**Jibu:** Tunauliza upapa, “Je, kweli ni wewe  ulibadilisha Sabato kuwa Jumapili?”

Anajibu, "Ndiyo, tulifanya hivyo kwa nini ishara, au alama yetu, ya mamlaka na nguvu."

Tunauliza, "Ungewezaje hata kufikiria kufanya hivyo?"

Ni swali muhimu. Lakini swali ambalo upapa huuwaulizi rasmi Waprotestanti ni lile muhimu zaidi. Tafadhali lisome kwa makini:

"Utaniambia kwamba Jumamosi ilikuwa Sabato ya Kiyahudi, lakini kwamba Sabato ya Kikristo imebadilishwa kuwa Jumapili, Imebadilishwa! Lakini ni nani amebadilisha? Ni nani aliye na mamlaka ya kubadilisha amri ya wazi ya Mungu Mwenyezi Wakati Mungu amesema? Naye alisema, Mtaiweka takatifu siku ya saba, ni nani basi atakayethubutu kusema, La, waweza kufanya kazi na pia mambo yako yote ya kilimwengu siku ya saba, lakini utaitakasa siku ya kwanza badala yake? Swali ambalo sijui unaweza kulijibuje wewe kama ni Mprotestanti, na ukaendelea bado kukiri kuwa unaenda kutokana na Maandiko yaani Biblia na Biblia pekee Yake na bado katika jambo hilo muhimu sana kama kutunza siku moja katika saba kama siku takatifu ukafanya kinyume kabisa na Neno Hilo lililo wazi kabisa ndani ya Biblia, na kuiweka siku nyingine mahali pa siku hiyo ambayo Biblia imeamuru. Amri ya kuitakasa siku ya saba ni mojawapo ya zile amri kumi unazoziamini kwamba zile tisa bado zina mashiko na zinakufunga kwa Yule Bwana aliyekupa zote zile kumi. Ni nani aliyekupa. mamlaka ya kuchezea ile ya nne basi? Ikiwa unapatana na kanuni zako mwenyewe, lakini unasema wewe bado unaifuata ile Kweli ya Biblia, na Biblia pekee, Je, unaweza kutoa sehemu fulani ya Agano Jipya ambamo amri hii ya nne imebadilishwa waziwazi." 11

11 Maktaba ya Mafundisho ya Kikristo: Kwa nini Huishiki Siku Takatifu ya Sabato? (London: Burns and Oates, Ltd.), uk. 3, 4.

Cha kusikitisha, Ukatoliki na Uprotestanti wote wanasimama na hatia mbele ya mahakama ya hukumu ya mbinguni kwa kukataa Sabato takatifu ya Mungu, ishara Yake Bwana takatifu ya utambulisho yaani inayomtambulisha Yeye kama Muumbaji, na Mmiliki.

**Viongozi wa kidini wanaopuuza Sabato takatifu ya Mungu watakabiliana na ghadhabu Yake.**

**6. Ni maonyo gani mazito ambayo Mungu ametoa kuhusu sheria Yake na ishara, au alama Yake?**

**Jibu:** A. Mungu anawaonya viongozi wa kidini dhidi ya kuwafanya watu wajikwae kwa kusema kwamba haijalishi kuzishika baadhi ya amri ( Malaki 2:7-9 ). Kwa mfano, baadhi ya wahudumu hufundisha, "Haijalishi ni siku gani wewe utaiweka utakatifu."

B. Mungu huwaonya watu wanaotaka wahudumu wao wahubiri hekaya za uongo badala ya Ukweli kuhusu sheria Yake ( Isaya 30:9 , 10 ).

C. Mungu huwaonya watu kuhusu kuifanya mioyo yao kuwa migumu dhidi ya Ukweli wa sheria Yake ( Zekaria 7:12 ).

D. Mungu anawaonya watu wanaosema ingeonekana kuwa "ajabu" kushika sheria ya Mungu kama Sabato, kwa mfano ( Hosea 8:12 ).

E. Mungu anasema kwamba msukosuko, misiba, matatizo, na taabu za dunia huja kwa sababu watu wanakataa kufuata sheria Yake, na hata wamejaribu kuibadilisha ( Isaya 24:4-6 ).

F. Mungu anawaonya viongozi wa kidini wanaokataa kuhubiri unabii wa nyakati za mwisho ( Isaya 29:10 , 11 ).

G. Mungu anawaonya kwa dhati viongozi wanaofundisha kwamba kwa kweli hakuna tofauti kati ya vitu vitakatifu (kama vile Sabato takatifu ya Mungu) na vitu vya kawaida (kama vile Jumapili) kwani watakabiliana na ghadhabu yake ( Ezekieli 22:26 , 31 ) .
Kipaji cha uso ni ishara ya akili. Watu watatiwa alama kwenye vipaji vya nyuso zao kwa kuadhimisha Jumapili kama siku takatifu.

**7. Ufunuo 13:16 inasema watu watapokea alama ya mnyama katika paji la uso au katika mkono. Hii ina maana gani?**

**Jibu:** Paji la uso linawakilisha akili ( Waebrania 10:16 ). Mtu atatiwa alama kwenye paji la uso kwa uamuzi wa kutunza Jumapili kama siku takatifu. Mkono ni ishara ya kazi ( Mhubiri 9:10 ). Mtu atatiwa alama mkononi kwa kufanya kazi katika Sabato takatifu ya Mungu au kwa kufuata sheria za Jumapili kwa sababu za kivitendo (kazi, familia, n.k.). Ishara, au alama, kwa Mungu au mnyama haitaonekana kwa watu. Wewe, mwenyewe kimsingi, utajitia alama kwa kukubali ama ishara au alama ya Mungu, ama Sabato, au alama ya mnyama, Jumapili. Ingawa alama hiyo haionekani kwa wanadamu, Mungu atajua ni nani aliye na alama ( 2 Timotheo 2:19 ).

**Mungu anataka watu Wake waache kukanyaga siku Yake takatifu.**

**8. Kulingana na Isaya 58:1, 13, 14 , ni ujumbe gani muhimu ambao Mungu huwapa watu Wake katika siku za mwisho?**
"Piga kwa sauti kubwa, usiache, paza sauti yako kama tarumbeta, uwahubiri watu Wangu kosa lao." "Kama ukigeuza mguu wako usiiache sabato, usifanye anasa yako katika siku Yangu takatifu, na kuiita sabato siku ya furaha, ... ndipo utakapojifurahisha katika Bwana." Isaya 58:1 , 13 , 14 .

**Jibu:** Anasema, waonyeshe "watu Wangu" kwamba wanatenda dhambi (bila hatia labda) kwa sababu wanaikanyaga siku Yangu takatifu, na waombe waache kuivunja Sabato Yangu ili niwabariki. Sema kwa sauti kubwa ili wakusikie!

Angalia malaika wa tatu wa Ufunuo 14:9-12 , ambaye analeta ujumbe kuhusu

alama ya mnyama, anazungumza kwa sauti kuu pia (mstari wa 9). Ujumbe ni muhimu sana kuuchukulia kama ni wa kawaida. Hakika hili ni suala la uzima au kifo. Yesu anasema kondoo Wake, au watu Wake, watamfuata atakapowaita. ( Yohana 10:16 , 27 ).

**Sheria zinapopitishwa kulazimisha ibada ya Jumapili, wale wanaotii watapokea chapa ya mnyama.**

**9. Je, wale watu wanaoabudu Jumapili (kama siku takatifu) wana alama ya mnyama sasa?**
**Jibu:** Hapana! Hakuna mtu atakayekuwa na alama ya mnyama hadi ibada ya Jumapili iwe suala la kulazimishwa na sheria. Wakati huo (mbele tu), wale wanaoamua kufuata mafundisho ya uongo ya mnyama na kuabudu siku ya Jumapili (siku takatifu ya bandia ya mnyama) watapokea alama ya mnyama.

Wale wanaomfuata Yesu na kutii ukweli Wake wataitunza siku ya Sabato kuwa takatifu na kupokea chapa yake. Wale wanaotarajia kukataa alama ya mnyama katika siku zijazo lazima waingie chini ya bendera ya Sabato ya Yesu sasa. Nguvu zake zinapatikana kwa wale wanaomtii ( Matendo 5:32 ). Bila Yeye, hatuwezi kufanya lolote ( Yohana 15:5 ). Kwake yote yanawezekana ( Marko 10:27 ).

**Ni wale tu walio na alama, au ishara ya Mungu katika vipaji vya nyuso zao ndio watakaoingia mbinguni.**

**10. Kulingana na kitabu cha Ufunuo, Yohana aliona nani hasa aliyekuwapo katika ufalme wa milele wa Mungu?**

**Jibu:** Jibu ni la tatu na la wazi kabisa:

A. Wale walio na alama ya Mungu, au ishara (Sabato Yake), katika vipaji vya nyuso zao ( Ufunuo 7:3 ).

B. Wale waliokataa kujitambulisha na yule mnyama au sanamu yake na waliokataa kuwa na alama au jina lake katika vipaji vya nyuso zao ( Ufunuo 15:2 ).

C. Watu ambao leo, na kwa umilele, wanafuata pale Yesu anapoongoza, wakimtumaini kikamilifu katika kila jambo ( Ufunuo 14:4 ). Hakuna njia nyingine.

**Kumfuata Yesu lazima kujumuishe kuitakasa Sabato Yake ya siku ya saba.**

**11. Yesu anawaambia nini watu leo?**
"Yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima." Yohana 8:1 .

**Jibu:** Ni ahadi ya ajabu iliyoje! Sisi tunapomfuata, hatutaishia gizani bali tutakuwa na Ukweli mtukufu. Hakuna jambo linaloweza kuwa la kusisimua zaidi! Zaidi ya hayo, kumfuata na kushika Sabato Yake kutaweka alama ya Mungu kwenye

vipaji vya nyuso zetu na kutulinda kutokana na mapigo ya kutisha ( Zaburi 91:10 ) ambayo yatawaangukia wasiotii ( Ufunuo sura ya 16 ). Pia inatutia alama kuwa tayari kuchukuliwa katika ujio wa pili wa Yesu. Mungu ametupa ulinzi, baraka na uhakikisho ulioje kwetu!

**Tahadhari ya Haraka**

Utagundua habari fulani yenye kustaajabisha unapojifunza Miongozo mitatu ya mwisho katika Miongozo ya Masomo yale tisa ambayo yanashughulikia jumbe za malaika watatu za Ufunuo 14:6-14 . Miongozo hii ya Masomo itaeleza (1) Sehemu ya Marekani katika pambano la mwisho la dunia, (2) jinsi makanisa na dini za ulimwengu zitakavyohusika, (3) na ni hali gani za ulimwengu zitakazochochea vita vya mwisho vya dunia, na (4) vita vya Shetani na mkakati wa ajabu wa kuhadaa mabilioni.

Labda unashangaa makanisa ya Kiprotestanti yanasemaje kuhusu madai ya upapa ya kubadilisha Sabato kuwa Jumapili. Nukuu zinazoonekana katika sehemu ya "Maswali Yako ya Fizra zako Yajibiwa" ya somo hili yatatoa majibu ya kushtua.

**12. Sasa nimeamua kuanza kushika Sabato Yake ya siku ya saba (Jumamosi) kama siku Yake takatifu na kumfuata popote anapoongoza.**

**Jibu:**

**Maswali ya Fikra au ya kucheua**
**1. Wahubiri na wachungaji wengine wanasema nini kuhusu Sabato na Jumapili? Jibu:**

2. Hapa kuna maoni mengi kuoka kwenye makanisa na mamlaka zingine kuhusu Sabato:

**Wabaptisti:** "Kulikuwa na Amri ya Mungu ya kuitakasa siku ya Sabato, lakini siku hiyo ya Sabato haikuwa Jumapili. ... Itasemwa, hata hivyo. , na kwa kuonyesha ushindi fulani, kwamba Sabato ilihamishwa kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza ya juma .... Je, Kumbukumbu ya jambo hilo la uhamishaji wa Sabato ya kweli inaweza kupatikana wapi? Haipo katika Agano Jipya --hakuna kabisa. hakuna ushahidi katika Maandiko wa mabadiliko ya utaratibu wa Sabato kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza ya juma." Dr. Edward T. Hiscox, mwandishi wa The Baptist Manual, katika karatasi iliyosomwa kabla ya mkutano wa wahudumu wa New York uliofanyika Novemba 13, 1893.

**Mkatoliki:** "Unaweza kusoma Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, na hutapata mstari mmoja unaoidhinisha utakaso wa Jumapili. Maandiko yanaamuru utunzaji wa kidini wa Jumamosi, siku ambayo sisi [Wakatoliki] hatuitakasi kamwe." James Cardinal Gibbons, The Faith of Our Fathers, toleo la 16, 1880, p. 111.

**Church of Christ:** "Mwishowe, tunao ushuhuda wa Kristo juu ya somo hili.

Katika Marko 2:27 , anasema: 'Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, na si mwanadamu kwa ajili ya Sabato.' Kutokana na fungu hili ni dhahiri kwamba Sabato haikufanywa kwaajili ya Waisraeli tu, kama vile Paley na Hengstenberg wangetaka tuamini, bali kwa ajili ya mwanadamu ... yaani kwa ajili ya jamii ya ubinadamu. ……na kwamba ilitolewa kwa Adamu, hata katika Edeni, kama mojawapo ya zile taasisi za kitambo ambazo Mungu aliziweka kwa ajili ya furaha ya watu wote." Robert Milligan, Mpango wa Ukombozi, (St. Louis, The Bethany Press, 1962), p. 165.

**Congregationalist:** "Sabato ya Kikristo [Jumapili] haimo katika Maandiko, na haikufitwa Sabato na kanisa la awali." Theolojia ya Dwight, Vol. 4, uk. 401.

**Episcopal/Anglican:** "Jumapili (Dies Solis, ya kalenda ya Kirumi, 'siku ya jua', kwa sababu wakfu kwa jua), siku ya kwanza ya juma, ilikubaliwa na Wakristo wa mapema kuwa siku ya ibada… . Hakuna kanuni za kuadhimishwa kwake zilizowekwa katika Agano Jipya, wala, kwa hakika, kutunzwa kwake, hata hakuna aliyeamuru." "Jumapili," A Religious Encyclopedia, Vol. 3, (New York, Funk na Wagnalls, 1883) p. 2259.

**Walutheri:** "Maadhimisho ya siku ya Bwana [Jumapili] hayakujengwa juu ya amri yoyote ya Mungu, bali yaliwekwa na mamlaka ya kanisa." Augsburg Confession of Faith, iliyonukuliwa katika Mwongozo wa Sabato ya Kikatoliki, Sehemu ya 2, Sura ya 1, Sehemu ya 10.

**Methodisti:** "Chukua suala la Jumapili. Kuna pendekezo katika Agano Jipya kuhusu jinsi kanisa lilikuja kutunza siku ya kwanza ya juma kama siku yake ya ibada, lakini hakuna fungu linalowaambia Wakristo kushika siku hiyo, au kuhamisha siku ya Sabato ya Kiyahudi hadi siku hiyo." Harris Franklin Rall, Wakili wa Kikristo, Julai 2, 1942.

**Taasisi ya Biblia ya Moody: *"Sabato ilikuwa ya lazima katika Edeni, na imekuwa ikitumika tangu wakati huo.* Amri** hii ya nne **huanza na neno 'kumbuka,' ikionyesha kwamba Sabato ilikuwepo tayari wakati Mungu alipoandika sheria kwenye mbao za mawe kule Sinai. *Je! watu wanawezaje kudai kwamba amri hii moja imebatilishwa wakati watakubali kwamba zile nyingine tisa bado zinafanya kazi au zina mashiko?"*** DL Moody, Kupimwa na Kutaka, uk. 47.

**Presbyterian:** "Mpaka, hapo itakapoweza kuonyeshwa kwamba sheria yote ya maadili imefutwa, Sabato itasimama .... Mafundisho ya Kristo yanathibitisha kudumu kwa Sabato." TC Blake, DD, Theology Condensed, uk. 474, 475.

**Pentekoste:** "'Kwa nini tunaabudu Jumapili? Je, Biblia haitufundishi kwamba Jumamosi inapaswa kuwa Siku ya Bwana?' … Inaonekana kwamba itatubidi kutafuta jibu kutoka kwa chanzo kingine zaidi y a Agano Jipya." David A. Womack, "Je, Jumapili ni Siku ya Bwana?" The Pentecostal Evangel, Agosti 9, 1959, No. 2361, p. 3.

**Encyclopedia:** " ***Jumapili*** lilikuwa jina lililopewa na wapagani kwa siku ya kwanza ya juma, kwa sababu ilikuwa siku ambayo waliabudu ***jua***, ... siku ya saba ilibarikiwa na kutakaswa na Mungu Mwenyewe, na .. . Yeye Anahitaji viumbe Vyake kuiweka takatifu Kwake. Amri hii ni wajibu wa ulimwengu wote na ni ya kudumu."

Eadie's Biblical Cyclopedia, 1872 ed., p. 561.

**Maswali au Kwizz**

**1. Watu wengi tayari wamepokea alama ya mnyama. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**2. Alama ya mnyama ni (1)**
_____ Nambari yako ya Hifadhi ya Jamii Security code.
_____ Jumapili kama siku takatifu.
_____ Namba ya mashine ya kupiga hesabu kwenye soko.

**3. Shirika la mnyama ambalo lina alama ni (1)**
_____ Umoja wa Mataifa.
_____ Upapa.
_____ Jumuiya ya Mataifa ya Ulaya.
_____ Tume ya Utatu.

**4. Alama ni halisi na itaonekana na wote. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**5. Mungu pia ana alama, au ishara, ya uwezo na mamlaka yake. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**6. Alama ya Mungu ya mamlaka ni (1)**
_____ Nambari ya siri ambayo hutolewa kwa kila Mkristo mwaminifu.
_____ Kunena kwa lugha.
_____ Utunzaji wa Sabato katika ukumbusho wa Uumbaji na utakaso.
_____ Ubatizo.

**7. Je, "mnyama" alijaribuje kubadili sheria ya Mungu? (2)**
_____ Kubadilisha Sabato (ya amri ya nne) kuwa Jumapili.
_____ Kufundisha kwamba si dhambi kufanya uzinzi.
_____ Kuondoa amri dhidi ya kuabudu sanamu.

**8. Katika unabii wa Biblia, miezi 42 ni ya muda gani? (1)**
_____ miaka 420 halisi.
_____ Miaka halisi mitatu na nusu.
_____ Siku 1,260 halisi.

_____ miaka 1,260 halisi.

**9. Alama ya mnyama itawekwa wapi? (2)**
_____ Mkononi.
_____ Mdomoni.
_____ Kwenye shavu.
_____ Katika paji la uso.

**10. Alama ya Mungu itawekwa wapi? (1)**
_____ Kwenye mkono.
_____ Katika paji la uso.
_____ Kwenye ulimi wa mtu.

**11. Ni ujumbe gani kati ya wale malaika watatu ambao ni onyo dhidi ya alama ya mnyama? (1)**
_____ Ujumbe wa malaika wa kwanza.
_____ Ujumbe wa malaika wa pili.
_____ Ujumbe wa malaika wa tatu.

**12. Mnyama huyo alijaribu kubadili nyakati za Mungu? (2)**
_____ Kusherehekea Mwaka Mpya kama likizo.
_____ Kubadilisha siku takatifu ya Mungu kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza ya juma.
_____ Kuweka saa za siku takatifu ya Mungu kama saa sita usiku hadi saa sita usiku badala ya machweo hadi machweo (alibadilisha masaa ya siku inapoonza, Biblia inasema siku inaanza jioni na kuishia jion!, yeye akabalishili na kusema inaanza saa sita ya usiku na kumalizika saa sita ya usiku, na ndiyo ratiba tunayoitumia leo).

**13. Yesu alitupa ujumbe wa onyo kuhusu alama ya mnyama. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**14. Ishara, alama, na muhuri vinatumika kwa kubadilishana katika Maandiko. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**15. Hakuna idhini ya kimaandiko ya kuadhimisha Jumapili kama siku takatifu. (1)**
_____ Kweli.
_____ Uongo.

**Marekani katika Unabii wa Biblia**

**Mwanamke Mwingine**

**Somo la 21**

Je, inaweza kuwa kweli kwamba Marekani ipo katika unabii wa Biblia - kabisa! Unapofikiria juu yake Marekani, linaeleweka kwamba ndilo taifa lenye nguvu na ushawishi mkubwa zaidi duniani na litakuwa na jukumu muhimu katika matukio ya mwisho ya kustaajabisha ya historia ya kufunga kwa ulimwengu. Lakini mambo mengi zaidi ya kushangaza yanakungoja, Biblia inapofunua jinsi taifa kuu la ulimwengu lilivyojitokea au lilivyoanza na kwa nini! Tafadhali soma Ufunuo 13:11-18 kabla ya kuanza mwongozo huu, kwa sababu mistari hii minane inatoa picha ya kinabii ya Marekani katika siku zijazo.

**Mnyama wa Ufunuo 13:1-10 anafananishwa na upapa.**

**1. Serikali kuu mbili za ulimwengu zinafananishwa katika Ufunuo sura ya**

**13. Serikali ya kwanza ni ipi?**

**Jibu:** Mnyama mwenye vichwa saba (Ufunuo 13:1-10) si mwingine ila upapa wa Kirumi. (Angalia Mwongozo wa Kusoma 15 kwa somo kamili juu ya mada hii.) Kumbuka kwamba hayawani/mnyama katika unabii wa Biblia hufananishwa na taifa au mamlaka za ulimwengu ( Danieli 7:17 , 23 ).

Mnamo 1798, Jenerali Berthier alitia jeraha baya upapa alipomchukua papa Pius mateka.

**2. Ni katika mwaka gani upapa ulitabiriwa kupoteza ushawishi na mamlaka yake ya ulimwengu?**

"Akapewa uwezo wa kufanya kazi hiyo miezi arobaini na miwili." Ufunuo 13:5 .

**Jibu:** Biblia ilitabiri kwamba upapa ungepoteza ushawishi na mamlaka yake ulimwenguni mwishoni mwa ile miezi 42. Unabii huu ulitimia mwaka 1798, wakati Jenerali Berthier wa Ufaransa, chini ya Napoleon alipomchukua papa mateka na mamlaka ya upapa ikapata jeraha lake la mauti. (Kwa maelezo kamili, ona Mwongozo wa 15.)

**Mnyama wa Ufunuo 13:11-18 anafananisha Amerika.**

**3. Ni taifa gani lilitabiriwa kutokea wakati ule ule upapa ulipokuwa ukipokea jeraha la mauti?**

"Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili kama mwana-kondoo, akanena kama joka." Ufunuo 13:11 .

Jibu: Utumwa wa papa uliotajwa katika mstari wa 10 ulifanyika mwaka wa 1798, na nguvu mpya (mstari wa 11) ilionekana ikitokea wakati huo. Marekani ilitangaza

uhuru wake mwaka wa 1776, ikapiga kura ya Katiba mwaka wa 1787, ikapitisha Mswada wa Haki yaani Bill of Rights mwaka wa 1791, na ikatambuliwa waziwazi kuwa mamlaka kuu ya ulimwengu kufikia 1798. Muda huo unalingana na Marekani kabisa na hakuna nchi nyingine imeweza kukidhi hivi vigezo isipokuwa Marekani. Hakuna mamlaka nyingine inayoweza imetimiza maneno haya, ukiipata tuambie nasi!

Unabii ulitabiri kwamba Amerika ingetokea kutoka eneo lisilo na makazi au watu.

"Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili kama mwana-kondoo, akanena kama joka." Ufunuo 13:11 .

Jibu: Utumwa wa papa uliotajwa katika mstari wa 10 ulifanyika mwaka wa 1798, na nguvu mpya (mstari wa 11) ilionekana ikitokea wakati huo. Marekani ilitangaza uhuru wake mwaka wa 1776, ikapiga kura ya Katiba mwaka wa 1787, ikapitisha Mswada wa Haki yaani Bill of Rights mwaka wa 1791, na ikatambuliwa waziwazi kuwa mamlaka kuu ya ulimwengu kufikia 1798. Muda huo unalingana na Marekani kabisa na hakuna nchi nyingine imeweza kukidhi hivi vigezo isipokuwa Marekani. Hakuna mamlaka nyingine inayoweza imetimiza maneno haya, ukiipata tuambie nasi!

**Unabii ulitabiri kwamba Amerika ingetokea kutoka eneo lisilo na watu wengi au makazi.**

**4. Ni nini maana ya mnyama "kupanda juu kutoka katika nchi"?**

**Jibu:** Taifa hili linainuka "kutoka katika nchi" badala ya kutoka majini kama yalivyofanya mataifa mengine yanayotajwa katika Danieli na Ufunuo. Tunajua kutokana na Ufunuo kwamba maji yanafananishwa na maeneo ya ulimwengu ambayo yana idadi kubwa ya watu. "Yale maji uliyoyaona, aketipo yule kahaba, ni jamaa na makutano na mataifa na lugha." Ufunuo 17:15 . Kwa hiyo, nchi kavu au dunia inawakilisha kinyume chake. Inamaanisha kwamba taifa hili jipya lingetokea katika eneo la ulimwengu ambalo lilikuwa na watu wachache sana kabla ya mwisho wa miaka ya 1700. Haukuweza kutokea kati ya mataifa yaliyosongamana na yanayohangaika ya Ulimwengu wa Kale yaani Asia, Afrika au Ulaya. Ilibidi itokee katika bara lenye watu wachache.

**5. Ni nini kinachofananishwa na pembe zake mbili zinazofanana na za wana-kondoo na pia kutokuwepo kwa taji?**

**Jibu:** Pembe zinawakilisha wafalme na falme, au serikali ( Danieli 7:24 ). 8:21 ). Katika kesi hii zinawakilisha kanuni mbili za utawala za Marekani: uhuru wa kiraia na wa kidini. Kanuni hizi mbili za uongozi pia zimeitwa "republicanism" (serikali isiyo na mfalme) na "Protestanti" (kanisa lisilo na papa). Mataifa mengine tangu nyakati za kale yalitoza watu kodi ili kuunga mkono dini ya serikali. Wengi wao pia walikuwa wamewakandamiza wapinzani wa kidini. Lakini Marekani ilianzisha jambo jipya kabisa: Uhuru wa kuabudu upendavyo bila kuingiliwa na serikali au udhibiti na ulinzi wa serikali. Kutokuwepo kwa taji kunamaanisha aina ya serikali ya jamhuri, badala ya ufalme. Pembe zinazofanana na za mwana-kondoo zinaashiria taifa lisilo na hatia, changa, lisilokandamiza, linalopenda amani na la kiroho. Yesu anatajwa kuwa Mwana-Kondoo mara 28 katika Ufunuo. Kwa hiyo serikali hii

mpya ilikuwa inajaribu kushikilia kanuni Zake. Hakuna mamlaka nyingine duniani ambayo ingeweza kutosheleza sifa na mpangilio wa wakati wa mnyama mwenye pembe za kondoo, isipokuwa Marekani.

Ujumbe Maalum: Lo! Jinsi tunavyotamani tungeishia hapa katika maelezo ya Yesu kuhusu Marekani, lakini hatuwezi, kwa sababu Marekani ilibadilika, haikufanya hivyo. Kinachofuata ni cha kutetemesha na kufadhaisha. Marekani kwa hakika ni nchi inayosisitiza kwa ukubwa uhuru Wake wa dhamiri, uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kutoa hotuba, biashara, na ulinzi ambao unatoa fursa zake za thamani, hisia zake za kusaidia wale wanaoonewa na mataifa mengine, huruma zake kama kiranja wa dunia kwa kuwashugulikia waonevu wa dunia na mwelekeo wake imara wa Kikristo. Marekani si mkamilifu katika haya lakini hata bado watu wengi kutoka nchi zingine wanaharakisha ili wawe raia wa Marekani kila mwaka, au wanapenda wawe raia wa Marekani. Ikiwa milango ya Marekani ingefunguliwa kwa upana, sehemu kubwa ya watu wa ulimwengu wangehamia Marekani mara moja wakifikiria wanakwenda "mbinguni iliyo duniani" kama wanavyoiona. Cha kusikitisha, nchi hiyo iliyobarikiwa sana itabadilika sana katika siku zijazo na kusababisha huzuni na ole zisizo na kifani kwa watu wa Mungu. Tunaripoti hili kwa utulivu, ila kwa wasiwasi mkubwa.

Marekani katika wakati wa mwisho itawalazimisha watu ama kuabudu au kuadhibiwa.

**6. Inamaanisha nini wakati unabii wa Ufunuo 13:11 unaposema Amerika itazungumza "kama joka"?**

**Jibu:** Kama tulivyojifunza katika Mwongozo wa Kusoma wa namba 20, joka ni Shetani, ambaye anafanya kazi kupitia serikali mbalimbali za dunia ili kusimamisha ufalme wake mbovu na kuliponda kanisa la Mungu kwa kuwatesa na kuwaangamiza watu Wake Mungu. Lengo la Shetani siku zote limekuwa ni kunyakua mamlaka na kiti cha enzi cha Mungu na kuwalazimisha watu kumwabudu na kumtii. (Angalia Mwongozo wa 2 kwa maelezo zaidi.) Kwa hiyo, "kuzungumza kama joka" kunamaanisha kwamba Marekani (chini ya ushawishi wa Shetani) katika siku za mwisho, itawalazimisha watu kuabudu kinyume cha dhamiri au kuadhibiwa.

Dini iliyoasi na serikali za kiraia zitaungana katika wakati wa mwisho kulazimisha dhamiri za watu.

7. **Marekani itafanya nini hasa kitakachoifanya izungumze kama joka?**

**Jibu**: Angalia mambo manne muhimu:

A. ***"Anatumia*** uwezo wote wa mnyama wa kwanza mbele yake." Ufunuo 13:12 . Marekani itakuwa mamlaka inayowatesa watu ambayo itawalazimisha watu kwenda kinyume na dhamiri zao, kama ilivyofanya Rumi ya kipapa ambayo imeonyeshwa katika nusu ya kwanza ya Ufunuo sura ya 13. B. "

Aifanya ***dunia*** na wote wakaao ndani yake kumwabudu mnyama wa kwanza, ambaye jeraha la mauti likapona." Ufunuo 13:12 . Marekani itaongoza mataifa ya ulimwengu katika kulazimisha ibada na utii kwa Mpinga Kristo wa upapa. Suala la mtanziko ni ibada siku zote. Je, Utamwabudu na kumtii nani? Je,

utamwabudu Kristo Muumba na Mkombozi wako, au Mpinga Kristo? Kila nafsi duniani hatimaye itamwabudu mmoja au mwingine. Mkakati mzima utaonekana kuwa ya kiroho sana. Miujiza ya ajabu itafanyika ( Ufunuo 13:14 , 15 ) ambayo itadanganya mabilioni (Ufunuo 13:3 ). Wale wanaokataa kujiunga na vuguvugu hili watachukuliwa kuwa watu wenye msimamo mkali na wasiomcha Mungu. Yesu anaita Amerika ya Kiprotestanti ya wakati wa mwisho "nabii wa uwongo" ( Ufunuo 19:20). 20:10 ), kwa sababu itaonekana kuwa ya kiroho na yenye kutegemewa lakini badala yake itakuwa ya kishetani katika mwenendo wake.

Haya yote yanaweza kuonekana kuwa hayawezekani, lakini maneno ya Yesu daima ni ya kutegemewa daima na ya Kweli ( Tito 1:2 ). Mungu a litabiri kuinuka na kuanguka kwa falme nne za ulimwengu na Mpinga Kristo (Danieli sura ya 2 na 7) wakati ambapo utabiri kama huo ulionekana kuwa wa ajabu na wa kushangaza. Lakini yote hayo yalitokea kwa usahihi kama ilivyotabiriwa. Onyo Lake kwetu leo kuhusu unabii ni, "Nimewaambia haya kabla hayajatokea, ili yatakapotokea mpate kuamini." Yohana 14:29 . .

C. ***"Akiwaambia*** wakaao juu ya nchi wamfanyie sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga, naye akaishi." Ufunuo 13:14 . Marekani itatengeneza sanamu ya mnyama huyo kwa kutunga sheria za kidini. Itapitisha sheria zinazohitaji ibada na kuwalazimisha watu ama kuzitii au kukabili kifo. Kitendo hiki ni nakala au taswira ya muungano wa kanisa na serikali ambao upapa ulitumia katika kilele cha mamlaka yake wakati wa Enzi za Kati, wakati huo mamilioni ya watu waliuawa kwa ajili ya imani yao. Amerika itaunganisha serikali ya kiraia na Uprotestanti ulioasi katika "ndoa" ambayo itaunga mkono upapa. Kisha itashawishi mataifa yote ya ulimwengu kufuata mfano wake. Hivyo, upapa utapata uungwaji mkono duniani kote.

D. ***"Na kuwafanya*** wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe." Ufunuo 13:15 . Marekani, ikiwa mkuu wa harakati hii ya kimataifa, itashawishi baadaye mataifa ya ulimwengu kuweka hukumu ya kifo ya ulimwengu mzima juu ya wote wanaokataa kumwabudu mnyama au sanamu yake. Jina lingine la muungano huu wa dunia nzima ni "Babylon the Great." (Mwongozo wa Somo la 22 utatoa taarifa zaidi.) Muungano huu wa ulimwenguni pote, katika jina la Kristo, utabadilisha nguvu za polisi badala ya ushawishi wa Roho Mtakatifu na utalazimisha ibada.

**8. Ni juu ya masuala gani hususani ambayo nguvu itatumiwa na hukumu ya kifo kutolewa?**

"Akapewa uwezo wa kuipa uhai ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya wote wasioisujudu sanamu ya yule mnyama wauawe. na wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au namba ya jina lake." Ufunuo 13:15-17 .

**Jibu:** Mambo ya mwisho ya mabishano yatakuwa ni kumwabudu na kumtii mnyama na kupokea chapa yake--Jumapili kama siku takatifu--dhidi ya kumwabudu na kumtii Kristo na kupokea chapa yake--Sabato Yake takatifu ya siku ya saba. (Kwa

maelezo zaidi, ona Mwongozo wa Kusoma 20.) Masuala yanapobainika na watu kulazimishwa ama kuabudu siku ya Jumapili na kuvunja Sabato au kuuawa, wale ambao watachagua Jumapili badala ya Sabato watakuwa, kimsingi, wanamwabudu mnyama. Watakuwa wamechagua kutii neno la kiumbe, ambaye ni mwanadamu, badala ya Neno la Muumba wao, Yesu Kristo. Hii hapa ndiyo kauli ya upapa iliyotolewa na mamlaka yake yenyewe: "Kanisa lilibadilisha Sabato kuwa Jumapili na ulimwengu wote unainama na kuabudu siku hiyo kwa utii wa kimya kwa mamlaka ya Kanisa Katoliki." Hartford Weekly Call, Februari 22, 1884.

Wakati wa Vita vya Pili vya Ulimwengu, stempu za mgao zilidhibiti uuzaji wa chakula, mafuta, matairi, na mahitaji mengine. Udhibiti kama huo unaweza kutumika tena kwa urahisi.

**9. Je, kweli serikali inaweza kudhibiti ununuzi na uuzaji?**
**Jibu:** Wakati wa Vita vya Pili vya Ulimwengu, ununuzi ulidhibitiwa kwa baadhi ya vitu (kama vile sukari, matairi, na mafuta ya magari) kwa kuhitaji stempu za malipo. Bila stempu au muhuri, pesa hazikuwa na thamani. Katika enzi hii za kompyuta nyingi, mfumo unaotegemea nambari yako ya Usalama wa Jamii (security code), unaweza kusanidiwa kwa urahisi. Isipokuwa kama umekubali kushirikiana na muungano wa kimataifa, nambari yako, ikipigwa/ikiingizwa kabla ya ununuzi, inaweza kukuonyesha kuwa hufai kununua au kuuza. Hatujui kwa hakika jinsi haya yote yatatovyokea. Lakini tunaweza kuwa na hakika kwamba yatatokea kwa sababu katika Ufunuo 13:16 , 17 , Mungu anasema yatatokea. Yeye akisema, daima tegemea jambo hilo litatimia! Mungu amesema yatatokea. Na hilo ni jibu tosha, kwa vile yote aliyosema yametokea, ama watu waliamini au hawakuamini, yalitokea

**Nguvu Mbili Zinazoibuka**
Ufunuo sura ya 13 iko wazi. Mataifa makubwa mawili yatatokea wakati wa mwisho: Marekani na Upapa. Marekani itaunga mkono upapa kwa kuongoza msukumo wa kuwalazimisha watu wa dunia kumwabudu mnyama (upapa) na kupokea chapa yake ama sivyo wakabiliane na kifo. Maswali mawili yanayofuata yatatathmini uwezo wa mataifa haya mawili makubwa.

***Upapa ni mamlaka yenye nguvu zaidi ya kidini na kisiasa duniani.***

**10. Upapa una nguvu na ushawishi gani leo?**
**Jibu:** Yeye ndiye mwenye nguvu zaidi za kidini na kisiasa ulimwenguni. Takriban kila nchi inayoongoza duniani ina balozi rasmi au mwakilishi wa serikali huko Vatikani. Zingatia ukweli ufuatao:

A. ***Upapa*** una ushawishi na nguvu nyingi sana hivi kwamba karibu kila nchi kuu hushauriana naye kabla ya kuchukua hatua kuu za kisera. "Makundi yake makubwa ya kidiplomasia yanadumisha uhusiano na zaidi ya mataifa 100." US News and World Report, Oktoba 30, 1978, p. 24.

B. ***Anachukua sifa*** ya kuangamia/kutokomea kwa ukomunisti, akisema kwamba Mariamu, mama yake Yesu, aliongoza mkakati wa papa ulioangusha ukomunisti.

"Handmaid or Feminist," Time, Desemba 30, 1991, ukurasa wa 64, 65.
C. ***Lengo la papa*** ni kuunganisha ulimwengu wa Kikristo chini ya uongozi wa upapa kufikia mwisho wa karne hii. Amefanya zaidi ya safari 40 duniani ili kuweka msingi wa lengo hili. Gene H. Hogberg, The Plain Truth, Novemba/Desemba 1989, ukurasa wa 24, 25.

D. ***Mwitikio wa ulimwenguni pote*** umekuwa karibu sana. Wakati wa mzozo wa Iraq, papa na rais wa Marekani wakati mwingine walijadili masuala ya dunia kila wiki kwa njia ya simu. US News and World Report, Agosti 13, 1990, p. 18.

E. Mnamo tarehe 7 Juni 1982, aliyekuwa Rais Ronald Reagan na Papa John Paul II walikutana kwa dakika 50 huko Vatikani na kuunda mpango wa kuondoa ukomunisti. Marekani ilisafirisha tani za vifaa vya kisasa vya mawasiliano hadi Poland (mahali pa kuanzia) ili kusaidia kueneza taarifa muhimu kwa raia. "The Holy Alliance," Time, February 1992, uk. 28, 31, 35.

F. Gorbachev alisema, "Kila kitu kilichotokea Ulaya ya Mashariki katika miaka ya hivi karibuni hakingewezekana bila juhudi za Papa na jukumu kubwa, ikiwa ni pamoja na jukumu la kisiasa ambalo alicheza katika uwanja wa ulimwengu." Mikhail Gorbachev, Toronto Star, Machi 9, 1992.

Upapa, ambao hapo awali ulitaja Waprotestanti kuwa "wazushi," sasa unawaita "ndugu waliojitenga" na kupendekeza kwa neema kwamba wote wafanye kazi na kusali pamoja kwa ajili ya amani na uwepo wa Mungu. Mamilioni ya Waprotestanti wanavutiwa sana na hilo. Kwa hakika, madhehebu kadhaa ya Kiprotestanti yamekuwa na mazungumzo rasmi na upapa ili kujaribu kusuluhisha tofauti zilizosababisha Matengenezo. Na wakati wa kusherekea miaka 500 ya Matengenezo ya Martin Luther, waprotestanti wengi walisema hakuna kupinga au "No Protesting again". Soma zaidi kuhusu maadhimisho haya ya miaka 500 Mwaka wa 2017, Oktoba 17, Tarehe ambayo Martin Luther aliweka hoja 95 kwenye huko Wittenberg.

**Amerika ndio nguvu kuu ya kijeshi duniani.**

**11. Marekani ina nguvu na ushawishi kadiri gani leo?**
**Jibu:** Marekani inachukuliwa kuwa nchi yenye nguvu ya kijeshi nambari moja na kitovu cha ushawishi. Zingatia yafuatayo:

A. " [Amerika ndiyo] nguvu kuu pekee iliyobaki kwenye sayari." "The UN Obsession," Time, May 9, 1994, p. 86.

B. "Hakuna matarajio katika siku zijazo za haraka za mamlaka yoyote ya kushindana na Marekani." Charles Krauthammer, "The Lonely Superpower", The New Republic, Julai 29, 1992, p. 23.

C. Yassir Arafat aliipa Amerika jina la "Rumi mpya" kwa sababu, kama vile Rumi ya zamani ilivyokuwa mamlaka kuu isiyopingika ya zama zake, Marekani sasa ndiyo nambari moja. Newsweek, Agosti 12, 1991, uku. 33.

D. “Nguvu za Amerika sasa zitaamua matukio yote makubwa ya ulimwengu.” Jim Hoagland, “Ya Mashujaa ...”, The Washington Post, Agosti 21, 1991, p. A-23.

Wakati kundi la Karl Marx lilipopindua serikali ya Ethiopia, Marekani iliombwa kujadiliana. Boris Yeltsin alipochukua madaraka kama rais wa Urusi mpya iliyojitegemea, alitembelea Marekani kwanza. Rais wa zamani wa USSR Mikhail Gorbachev aligeukia Marekani katika shida yake. Wakati Kuwait ilipovamiwa, serikali yake iliitaka Marekani kutoa msaada. Vita vilivyoongozwa na Marekani dhidi ya Iraki viliungwa mkono na takriban dunia nzima.
Mwandishi wa Redio ya Umma ya Taifa alimwita rais wa Marekani “rais wa dunia.” Sasa tuna “muundo usio wa kawaida wa ulimwengu wenye nguvu moja, Marekani, katika kilele cha mfumo wa kimataifa.” Krauthammer, Jamhuri Mpya, p. 23.

**Mataifa mengi au tuseme yote ya ulimwengu sasa yanatazamia Marekani kwa ajili ya ulinzi na usaidizi.**

**12. Ni wazi kwamba ushawishi na mamlaka ya Marekani na upapa yanaongezeka kwa kasi. Ni mambo gani mengine yanayoweza kusaidia kuweka msingi wa sheria ya ulimwenguni pote ya kuwaua wale wanaokataa kukiuka dhamiri?**

**Jibu:** Hatuwezi kutaja kwa yakini, lakini mambo machache yanayojitokeza ni haya yafuatayo:

A. Shughuli ya magaidi.
B. Machafuko na kuongezeka kwa uhalifu na uovu.
C. Vita vya madawa ya kulevya.
D. Ajali kubwa ya kiuchumi.
E. UKIMWI na magonjwa mengine ya mlipuko.
F. Vitisho vya nyuklia kutoka kwa mataifa yenye msimamo mkali.
G. Ufisadi wa kisiasa.
H. Ukosefu mkubwa wa haki unaofanywa na mahakama.
I. Unyanyasaji wa ustawi.
J. Kuongeza kodi.
K. Ponografia, ushoga na uasherati/uzinzi wa kutisha.
L. Maafa ya kutisha ya kimataifa.
M. Vikundi vya mapinduzi au siasa kali ‘Radical’ “maslahi maalum” vikundi.
N. Mgogoro wa utoaji mimba.

Msukosuko dhidi ya ufisadi, uasi-sheria, ubaguzi wa rangi au dini, ukosefu wa maadili, kuruhusu mambo ya uovu kufanyika na kuachia mambo yafanywe kiholela‘permissive”, ukosefu wa haki, umaskini, viongozi dhaifu wa kisiasa na wasiofaa, na ole nyingi zinazofanana na hizo zingeweza kuchochea kwa urahisi matakwa ya sheria kali, hususani zitekelezwe kwa uthabiti.

**13. Hali za ulimwengu zinapokuwa mbaya zaidi, Shetani atafanya nini ili kuwadanganya watu wengi?**
"Naye afanya maajabu makubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu, na kuwapoteza wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizokuwa nazo kuzifanya mbele ya macho ya watu. mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi wamfanyie sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga, naye akaishi." Ufunuo 13:13 , 14 .

**Jibu:** Marekani itapata uamsho ghushi/feki, duniani kote na itasisitiza kwamba sheria za kidini zipitishwe ili kulazimisha kila mtu kushiriki. (Hii inawakilishwa na "sanamu ya mnyama" katika Ufunuo 13:14 .) Watu watalazimika kupuuza Sabato takatifu ya siku ya saba ya Mungu na badala yake waabudu katika siku "takatifu" ya mnyama huyo—Jumapili. Baadhi pia watatii kwa sababu za kijamii au kiuchumi. Hali za ulimwengu zitakuwa zisizovumilika hivi kwamba vuguvugu la ulimwenguni pote la kaulimbi ya "Turudi kwa Mungu na sala", pamoja na wote wanaojiunga katika ibada na sala Jumapili, litaonekana kuwa suluhisho pekee. Shetani ataudanganya ulimwengu kuamini kwamba ni lazima wakubali Ukweli wa Biblia na kuitakasa Jumapili. Lakini kwa kweli, kutii na kumwabudu mnyama huyo kutawafungia watu nje ya ufalme wa Mungu. Si ajabu kwamba Yesu adokeza suala kama hilo katika Ufunuo juu ya kumwabudu mnyama na kupokea alama yake!
Katika siku za mwisho duniani, ujumbe wa Mungu wa tumaini la wakati wa mwisho utamfikia kila mtu.

**14. Ingawa kupendezwa na uamsho huo bandia kunaongezeka, ni nini kitakachokuwa kikitukia kwa uamsho wa Kweli wa ulimwenguni pote unaofadhiliwa na watu wa Mungu wa nyakati za mwisho?**
**Jibu:** Biblia inasema ulimwengu wote "utaangazwa" na utukufu Wake ( Ufunuo 18:1 ). Kila mtu duniani atafikiwa ( Marko 16:15 ) kwa ujumbe wa Mungu wa nyakati za mwisho, wenye sehemu/mambo matatu wa Ufunuo 14:6-14 . Kanisa la Mungu la siku za mwisho litakua kwa kasi ya ajabu wakati mamilioni ya watu wanapojiunga na watu wa Mungu na kukubali toleo Lake la wokovu kwa neema ya bure na imani katika Yesu, ambayo inawabadilisha kuwa watumishi Wake watiifu. Watu wengi na viongozi kutoka nchi zote za ulimwengu watakataa kumwabudu mnyama huyo na kukumbatia mafundisho yake ya uwongo. Badala yake, watamwabudu na kumtii Yesu pekee. Kisha watapokea ishara Yake takatifu ya Sabato, au alama, katika vipaji vya nyuso zao ( Ufunuo 7:2 , 3 ), hivyo kuwatia muhuri kwa umilele.

**Kupanda ngazi juu kwa kazi ya Mungu Kunaongezeka na Kukasirisha Mwenendo wa Uamsho wa Bandia**
Kupanda kuelekea juu kunakoendelea kati ya watu wa Mungu kutawakasirisha wale wenye harakati ghushi/feki. Viongozi wake watakuwa na hakika kabisa kwamba wale wanaokataa kushirikiana na uamsho wa uwongo wa ulimwenguni pote ndio sababu ya ole zote za ulimwengu ( Danieli 11:44 ). Watawanyima sifa za kununua na kuuza bidhaa au hata chakula (Ufunuo 13:16 , 17 ), lakini Mungu atawalisha watu Wake ( Isaya 33:16 ) na kuwalinda ( Zaburi 34:7 ).

**Akiwa katika muujiza wake mkuu, Shetani atajifanya kuwa Yesu.**

**15. Kwa kukata tamaa, muungano unaoongozwa na Marekani baadaye utaamua kutoa hukumu ya kifo kwa maadui wake (Ufunuo 13:15). Andiko la Ufunuo 13:13, 14 linasema viongozi wake watafanya nini ili kuwasadikisha watu kwamba Mungu Yuko pamoja nao?**

**Jibu:** Watafanya miujiza ya kusadikisha watu hivi kwamba kila mtu atatekewa, isipokuwa watu waaminifu wa Mungu wa wakati wa mwisho hawatashawishiwa ( Mathayo 24:24 ). Wakitumia roho (au malaika walioanguka) wa Shetani ( Ufunuo 16:13 , 14 ), watajifanya wapendwa wa watu waliokufa kupitia uchawi -dini ya umizimu ( Ufunuo 18:23 ) na pengine hata kujifanya kuwa manabii na mitume wa Biblia. Hawa wanaosema uwongo ( Yohana 8:44 ), roho ovu, bila shaka watadai kwamba Mungu amewatuma kuwahimiza wote kushirikiana.

**Shetani Atokea Kama Kristo na Malaika zake Wanajifanya Kama Wahudumu Wakristo**

Malaika wa Shetani watatokea pia kama makasisi wanaomcha Mungu, na Shetani atatokea kama malaika wa nuru ( 2 Wakorintho 11:13-15 ). Kama muujiza wake mkuu wa kukata shoka, Shetani atadai kuwa Yesu ( Mathayo 24:23 , 24 ). Shetani, huku akijifanya Kristo, atadai kwa urahisi kwamba yeye aliibadilisha Sabato kuwa Jumapili na kuwahimiza wafuasi wake kuendelea na uamsho wao wa ulimwenguni pote na kushikilia siku yake "takatifu", Jumapili.

**Mabilioni Yanadanganywa**

Mabilioni, wakiamini kwamba Shetani ni Yesu, watainama miguuni pake na kujiunga na harakati za kughushi/feki. "Ulimwengu wote ulimfuata mnyama kwa kustaajabisha." Ufunuo 13:3 , NEB.* Udanganyifu huo utakuwa na matokeo makubwa sana. Lakini watu wa Mungu wa wakati wa mwisho hawatadanganywa, kwa sababu wanapima kila kitu kutokana na Biblia ( Isaya 8:19 , 20 ) 2 Timotheo 2:15 ). Biblia inasema sheria ya Mungu haiwezi kubadilishwa ( Mathayo 5:18 ). Pia inasema kwamba wakati Yesu atakaporudi, kila jicho litamwona ( Ufunuo 1:7 ) na hataigusa dunia bali atabaki katika mawingu na kuwaita watu Wake wakutane Naye hewani ( 1 Wathesalonike 4:16 , 17 ) )

**16. Tunawezaje kuwa salama kutokana na udanganyifu wenye nguvu wa wakati wa mwisho?**
**Jibu:** A. Lipime kila fundisho la Biblia ( 2 Timotheo 2:15 Matendo 17:11 Isaya 8:19 , 20 ).

B. Fuata Ukweli jinsi Yesu anavyoufunua. Yesu anaahidi kwamba wale wanaofanya mapenzi Yake hawataishia katika makosa kamwe ( Yohana 7:17 ).

C. Kaa karibu na Yesu kila siku ( Yohana 15:5 ).

**Kumbuka:** Huu ni Mwongozo wa sita wa Mafunzo katika mfululizo wetu wa tisa kuhusu jumbe za malaika watatu. Mwongozo unaofuata wa Masomo utaonyesha jinsi makanisa ya Kikristo na dini nyingine duniani kote yatakavyohusiana na matukio ya wakati wa mwisho.

**17. Je, uko tayari kumwabudu na kumtii Yesu hata ikimaanisha dhihaka, mateso, na hatimaye hukumu ya kifo?**

**Jibu:**

**Maswali ya Kucheua na kufikiri**

**1. Je, ni haki kweli kwamba, katika mgogoro wa mwisho, watu ambao hawajawahi kusikia Ukweli wa Mungu na bila wao kujua wanaweza kuchagua injili bandia na hivyo kupotea.**

Hakuna mtu atakayekabili mgogoro wa mwisho bila kupata nafasi ya kusikia kwanza ( Marko 16:15 ) na kuelewa ( Yohana 1:9 ) Ujumbe muhimu wa Mungu wenye sehemu tatu kwa leo ( Ufunuo 14:6 ). Watu watachagua kupokea alama ya mnyama wakati huo kwa sababu tu hawataki kulipa gharama ya kumfuata Kristo. Watu watachagua kupokea alama ya mnyama wakati huo kwa sababu tu hawataki kulipa gharama ya kumfuata Kristo. Hakuna ambaye hatapewa nafasi ya kuelewa mambo, na hivyo kufanya uchaguzi ulio mwema. Mungu ni Mungu wa haki, si dhalimu, Naye anatupenda kuliko tunavyojipenda na wale ambao sisi tunawapenda, Yeye anawapenda zaidi yetu. Tukiwa na hili mawazoni, tunajua kabisa kwamba kila mtu atapewa nafasi, na mlango wa rehema Mungu ataufunga tu pale ambapo kutakuwa hakuna tofauti katika chaguzi za watu, na hivyo, hakuna haja ya kungojea tena, kwani kila mtu ameshafanya uchaguzi, na hivyo hata akilazimishwa kwenda mbinguni, ataona ni mahali pabaya sana yeye kuwapo, na patamkera, patamchukiza na kumhuzunisha. Hatapenda kuimba nyimbo tamu pale, hatapenda kutendea watu na Mungu mema, nawe unajua kabisa hutapenda kwenda mbingu ambayo mtu atakuja pale ulipopumzika ukila matunda na akuchape kiboko! Dhambi haitainuka tena kule, Nahum 1:9 kwa vile itakuwa imeteketezwa hapa duniani na shetani na wafuasi wake. Mungu ni Mwenye rehema kupita mwingine yoyote. Hili limungunye taratibu, acha lizame mawazoni maana ni takaribani mara 570 tu ndiyo Maandiko yamezungumzia kuhusu hasira Yake, ila maelfu ya mafungu yamezungumza kuhusu upendo Wake, ambao ni wa milele, Naye ni UPENDO, siyo ana upendo, la! Ni UPENDO! Upendo unahusisha tabia zaidi ya 26, kama vile upole, wema, fadhila, uvumililivu, maneno ya mwanadamu hayatoshi kueleza upendo wa Mungu ambao unaitwa Agape. Mungu atujalie kuwa kule mbinguni ambapo nasi upendo wetu utaendelea kukua milele, ujuzi wetu wa mema na Maandiko utaendelea kukua milele, mahusiano yetu na Mungu yataendelea kukua milele. Maisha yetu yatalinganishwa na yale ya Mungu kwa miaka, yaani yatakuwa ya MILELE. Hasira ya Mungu ni kuhusu uovu, nawe pia unajua unapoona mtu unayempenda anatendewa uovu, hakika utachukua hatua, na kama una uwezo usingependa mtu huyo awe karibu na zimwi anayetesa watu tena.

**2. Je, ni vita gani vya Har–Magedoni vinavyozungumziwa katika Ufunuo 16:12-16 ? Je hii vita itapigwana lini na wapi?**

Vita vya Har–Magedoni ni vita vya mwisho kati ya Kristo na Shetani. Itapiganwa duniani na itaanza kabla tu ya mwisho wa nyakati. Vita vitakatizwa na ujio wa pili wa Yesu. Vita itaanza tena baada ya miaka 1,000, wakati waovu watakapozingira mji mtakatifu kwa matumaini ya kuuteka. Vita hivi vitamalizwa/vitafungwa wakati Mungu atakaponyesha moto kutoka mbinguni juu ya waovu na kuwaangamiza ( Ufunuo 20:9 ). (Mwongozo wa 12 wa Somo unaelezea miaka 1,000 kwa undani.)

**Neno "Har–Magedoni" Linamaanisha Nini?**

Har–Magedoni ni jina la Kufanisha na vile "vita vya siku ile kuu ya Mungu Mweza-Yote" kati ya Kristo na Shetani ambamo mataifa yote ya ulimwengu yatahusika ( Ufunuo 16:12-16 , 19 ). "Wafalme wa mashariki" ni Mungu Baba na Mungu Mwana. "Mashariki" katika Biblia hufananisha ufalme wa mbinguni wa Mungu ( Ufunuo 7:2 Ezekieli 43:2 Mathayo 24:27 ).
Katika vita hivi vya mwisho, karibu ulimwengu wote utaungana ( Ufunuo 16:14 ) kupigana na Yesu, Mwana-Kondoo, na watu wake ( Ufunuo 17:14 ) 19:19 ). Kusudi lao litakuwa kuwaangamiza wote wanaokataa kumwabudu mnyama na kukubali alama yake ( Ufunuo 13:15-17 ).

**Udanganyifu Hufuata Kukataliwa**

Watu wanaokataa kuukubali ujumbe wa Mungu wenye sehemu/mambo matatu wa siku za mwisho (ingawa wanajua ni kweli), watadanganyika sana ili wauamini uwongo ( 2 Wathesalonike 2:10-12 ). Wataanza kuamini kwa kwa unyofu na upotofu kwamba wao wanaunga mkono ufalme mkuu wa Mungu wanapojaribu kuwaangamiza watu wa Mungu. Watawaona watakatifu kuwa ni watu washupavu waliodanganyika bila tumaini ambao wanaangamiza ulimwengu mzima kwa kukataa kwao kushirikiana katika uamsho huo ghushi.

**Kuja kwa Yesu Mara ya Pili Kutasimamisha Vita**

Vita vyenyewe vitakuwa ulimwenguni kote. Serikali zitajaribu wakati uleule kuwaangamiza watu wa Mungu, lakini Mungu ataingilia kati. Mto wa mfano Frati utakauka ( Ufunuo 16:12 ). Maji yanawakilisha watu ( Ufunuo 17:15 ). Kukauka kwa mto Frati kunamaanisha kwamba watu ambao wamekuwa wakimuunga mkono mnyama (ufalme wa Shetani) wataondoa kumtegemea kwao kwa ghafula. Msaada wa mnyama utakauka. Muungano wake wa washirika ( Ufunuo 16:13 , 14 ) utasambaratika ( Ufunuo 16:19 ). Kuja kwa Yesu mara ya pili kutasimamisha vita hivi na kuwaokoa watu wake ( Ufunuo 6:14-17 16:18-21 19:11-20 ).

**Vita Vinaanza tena Baada ya Miaka 1,000**

Baada ya ile miaka 1,000, Shetani atajitokeza waziwazi akiwa kiongozi wa majeshi dhidi ya Mungu na watu Wake. Ataanza vita tena dhidi ya Mungu anapojaribu

kuuteka mji mtakatifu. Kisha Shetani na wafuasi wake wataangamizwa kwa moto kutoka mbinguni (ona Miongozo ya Masomo 11 na 12). Kila mfuasi wa Shetani ataangamizwa. Kila mfuasi wa Yesu ataingia katika ufalme Wake wa milele.

**3. Biblia inasema, "Wakati unakuja ambapo kila mtu akiwaua atadhani kwamba anamtumikia Mungu." Yohana 16:2. Je, unafikiri hilo litatimizwa kihalisi katika wakati wetu?**

Ndiyo. Muungano wa siku za mwisho wa serikali na dini za ulimwengu hatimaye utapoteza huruma zote kwa watu wa Mungu, kwa wale wanaokataa kujiunga na uamsho wa bandia au kuchukua ishara yake (ibada ya Jumapili). Watahisi kwamba miujiza ya ajabu inayoandamana na uamsho wao inathibitisha uhalali wake—miujiza kama vile wagonjwa kuponywa au watu wenye sifa mbaya sana wanaomchukia Mungu, wacheza filamu wasio na maadili, viongozi wa biashara za madawa ya kulevya, na kisha wahalifu wanaojulikana sana kuongoka. Muungano huo utasisitiza kwamba hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kuharibu uamsho huu wa dunia nzima ambao unavuta dini zote. Kila mtu atahimizwa kuweka kando hisia za kibinafsi na "mafundisho ya ushupavu" kama ya (Sabato, kwa mfano) na kujiunga na ulimwengu wote katika uamsho wake wa dhati kwa amani na udugu. Kila kitu kingine isipokuwa uamsho kitachukuliwa kuwa kidogo tu. Wale ambao hawatakubali kushirikiana watachukuliwa kuwa wasio waaminifu, wasio na uzalendo, machafuko ya kutokuwa na uongozi au machafuko (anarchist) na, hatimaye, wataonekana washupavu na watu wa hatari ambao hawapaswi kuvumiliwa. Siku hiyo, wale wanaowaua watu wa Mungu watahisi kwamba wanamfanyia Mungu upendeleo/ feva (favor).

**4. Ninapojifunza unabii wa Danieli na Ufunuo, inaonekana dhahiri kwamba adui wa Kweli daima ni ibilisi. Je, Unakubali hilo?**

Hakika Kabisa! Uko sahihi kwa asilimia 100! Shetani ni adui wa halisi/kweli siku zote. Shetani hutumia viongozi na mataifa ya dunia kuwaumiza watu wa Mungu na hivyo kuleta huzuni kwa Yesu na Baba. Tunasahau kwa urahisi sana kwamba Shetani ni adui. Yeye ndiye anayehusika na uovu wote. Hebu tumlaumu na tuwe makini jinsi tunavyohukumu na kulaani watu au mashirika yanayoumiza watu wa Mungu na kanisa. Wakati mwingine hawana habari au hata hawajui kabisa kwamba wanadhuru mtu yeyote. Lakini hiyo si kweli kamwe kuhusu Shetani. Yeye daima anafahamu kikamilifu kwamba anamwumiza mtu. Anamuumiza Mungu na watu Wake kwa makusudi. Sisi ni walengwa wa upendo Wake Bwana na hivyo tuwe na moyo mkuu, tukikesha kwa maombi.

**5. Je, kifo cha papa au kuchaguliwa kwa rais mpya kungeathirije unabii wa Marekani katika Ufunuo 13:11-18?**

Unabii huo utatimizwa bila kujali nani ni papa au rais. Rais mpya au papa mpya anaweza kuharakisha kwa muda au kupunguza kasi ya jambo hilo kutimia, ila matokeo ya mwisho yanathibitishwa na unabii wa Biblia.

**6. Je, manyama au hayawani-mwana-kondoo wa Ufunuo 13:11-18 na "nabii wa uwongo" wa Ufunuo 16:13 wana nguvu sawa?**

Ndiyo. Katika Ufunuo 19:20 , ambapo Mungu anataja uharibifu wa mnyama Mpinga

Kristo, Yeye pia inahusu kuangamizwa kwa nabii wa uongo. Katika kifungu hiki, Mungu anamtambulisha nabii wa uwongo kama mamlaka ambayo "yaliyofanya miujiza" mbele ya mnyama na "kuwapoteza wale waliopokea chapa ya mnyama, na wale walioisujudia sanamu yake." Hili ni rejeleo la wazi kabisa la utendaji wa mnyama aliyeonekana mpole, yaani-mwana-kondoo, ambao unafafanuliwa katika Ufunuo 13:11-18 . Katika Mwongozo huu wa Somo tumemtambua mnyama mwenye pembe za mwana-kondoo kama Marekani. Kwa hiyo mnyama mwenye pembe za kondoo na nabii wa uwongo ni wazi ni nguvu zilezile.

**Maswali -Kwizz**

**1. Marekani inafananishwa na nini katika unabii wa Biblia na (1)**
_____ Mtu aliyevaa nguo nyekundu, nyeupe na bluu.
_____ Tai mwenye kompyuta mgongoni.
_____ Mnyama mwenye pembe mbili kama mwana-kondoo.

**2. Pembe mbili zinawakilisha nini? (1)**
_____ Utajiri na uwezo wa kijeshi.
_____ Benjamin Franklin na George Washington.
_____ Uhuru wa kiraia na wa kidini.

**3. "Kupanda juu kutoka katika nchi" kunamaanisha nini? (1)**
_____ Kwamba Wamarekani wangependa kuishi katika nchi hiyo.
_____ Kwamba nchi hii mpya ingetokea katika eneo lenye watu wachache.
_____ Kwamba baadhi ya Wamarekani wa mapema wangekuwa wakaaji wa mapangoni.

**4. Katika unabii huu, pembe kama za mwana-kondoo inamaanisha kwamba Marekani (1)**
_____ itakuwa na soni usoni na kuzuiliwa.
_____ Itakuwa nchi ya kufuga kondoo.
_____ Itainuka kama taifa linalopenda amani, taifa la kiroho.

**5. Ni saa ngapi unabii wa Ufunuo sura ya 13 unaonyesha Amerika ingetokea? (1)**
_____ 1492.
_____ 1798.
_____ 1620.

**6. Ufunuo sura ya 13 inaonyesha kwamba Marekani hatimaye ingezungumza "kama joka." Hii ina maana gani? (1)**
_____ Watu wake wangekuwa na hasira na wagumu kuelewa.
_____ Angetumia silaha za kurusha mioto ya uharibifu.
_____ Atawalazimisha watu kuabudu kinyume cha dhamiri au kukabili kifo.

**7. Alama ya Mungu, ishara, au alama ya nguvu ni (1)**
_____ Mwana-kondoo.
_____ Mnyama mwenye pembe mbili.
_____ Sabato, siku takatifu ya Mungu.

**8. Marekani itafanyaje "sanamu ya mnyama"? (1)**
_____ Kwa kutengeneza na kuuza picha nyingi za mnyama.
_____ Kwa kutengeneza sanamu ya mnyama ili ionyeshwe huko Washington, DC
_____ Kwa kuunda mchanganyiko wa kanisa na serikali (iliyochorwa baada ya upapa katika kilele cha mamlaka yake) ambayo itahalalisha mazoezi ya kidini.

**9. Andiko la Ufunuo 13:15–17 linasema kwamba watapewa adhabu gani wale wanaokataa alama ya mnyama? (2)**
_____ Hairuhusiwi kununua au kuuza.
_____ Watafukuzwa mtandaoni.
_____ Watauawa.
_____ Watalazimishwa kuomba msamaha wa kibinafsi kwa mnyama.

**10. Ni serikali gani mbili za kidunia zitakuwa na ushawishi mkubwa zaidi wakati wa mwisho? (2)**
_____ Ilihuisha Ulaya.
_____ Japan.
_____ Uchina.
_____ Marekani.
_____ Upapa.

**11. Ni mambo gani yanayosema Ukweli kuhusu vita vya Har–Magedoni? (6)**
_____ Ni vita vya mwisho duniani.
_____ 'Wafalme wa mashariki' ni Japan na Uchina.
_____ Kusudi la mnyama katika vita ni kuwaangamiza watu wa Mungu.
_____ Itakuwa duniani kote.
_____ Inaanza kabla ya ujio wa pili wa Yesu na kuishia baada ya waovu kuuzunguka mji mtakatifu mwishoni mwa miaka 1,000.
_____ Armageddon ni jina la mfano la vita vya mwisho kati ya Kristo na Mpinga Kristo, au Shetani.
_____ Kukausha Mto Frati kunamaanisha kuwa mnyama, au Mpinga Kristo, na hatimaye atapoteza kuungwa mkono na wengi wa wafuasi wake.
_____ Itapiganwa katika Palestina pekee.

**12. Je, uamsho wa Kweli wa Mungu wa nyakati za mwisho utafanikiwa kwa kiasi gani? (2)**
_____ Ulimwengu wote utaongoka.
_____ Kila mtu duniani atasikia ujumbe.
_____ Mamilioni wataukubali.
_____ Hautafanikiwa. Ibilisi ataizuia.

**13. Je, harakati za siku za mwisho za kughushi zitafanikiwa kwa kiasi gani? (1)**
_____ Nchi nyingi hazitaunga mkono.
_____ Litafanikiwa Marekani na Ulaya pekee.
_____ Kila mtu duniani isipokuwa watu wa Mungu wa wakati wa mwisho watajiunga na kuunga mkono jambo hilo.

**14. Miujiza ya ufufuo huo bandia itakuwa na nguvu kiasi gani? (2)**
_____ Sio sana; watu wataziona kama ni hila tu.
_____ Ina uwezo wa kutosha kudanganya karibu ulimwengu mzima.
_____ Wasio na shahada pekee ndio watakaowaangukia.
_____ Nguvu sana hivi kwamba wateule wa Mungu pekee ndio watakaoepuka udanganyifu.

**Mwanamke Mwingine**

**Somo la 22**

Kila ndoa lazima itegemee uaminifu - na vivyo hivyo katika muungano wetu na Kristo, lazima tubaki waaminifu Kwake na Neno Lake. Ufunuo unazungumza juu ya bibi-arusi wa kweli wa Kristo, lakini kuna mwanamke mwingine ambaye anajaribu kuwapotosha waamini mbali na Neno la Mungu. Ufunuo una ujumbe wenye kushtua kuhusu Babeli, yule mwanamke mwingine. Babiloni imeanguka, na watu wa Kristo lazima waepuke hirizi zake au waangamie! Hivyo huanza sehemu ya pili ya ujumbe wa malaika watatu. Hapa utajifunza utambulisho halisi wa Babeli wa kiroho na kujifunza jinsi ya kuepuka kudanganywa na uzuri wake mbaya ... ni nini kinachoweza kuwa muhimu zaidi?

Katika kitabu cha Ufunuo, Mungu anamwita mwanamke huyu "Babeli."

**1. Yesu anafananishaje Babiloni katika kitabu cha Ufunuo?**
"Nitakuonyesha hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi." "Nikaona mwanamke ameketi juu ya mnyama mwekundu sana, mwenye kujaa majina ya makufuru, mwenye vichwa saba na pembe kumi. kikombe mkononi mwake, kilichojaa machukizo na machafu ya uasherati wake; Ufunuo 17:1 , 3-5 .

**Jibu:**
Katika Ufunuo 17:1-6 , Yesu anafananisha Babeli kama kahaba aliyevaa nguo nyekundu na zambarau. Ameketi juu ya hayawani-mwitu mwenye rangi nyekundu, ambaye ana vichwa saba na pembe 10 na kuketi juu ya maji mengi.

**2. Mwanamke safi wa ufananisho wa Ufunuo sura ya 12 ni nani?**
**Jibu:** Mwanamke safi, aliyevikwa jua, anaonyeshwa kwenye Ufunuo 12:1-6 . Tulijifunza katika Mwongozo wa 20 kwamba mwanamke huyu safi anafananisha kanisa safi la Mungu ambalo ni mwaminifu kwa mpenzi wake, Yesu. Tutajifunza Ufunuo sura ya 12 kwa kina katika Mwongozo wa 23 wa Somo.

**3. Kahaba anawakilisha nini katika unabii wa Biblia?**
"Uujulishe Yerusalemu machukizo yake." "Uliutumainia uzuri wako, ukafanya uzinzi." Ezekieli 16:2 , 15 .

**Jibu:** Kama vile mwanamke safi anavyoashiria kanisa safi ambalo ni mwaminifu kwa Yesu, vivyo hivyo mwanamke mchafu anawakilisha kanisa chafu, au lililoanguka, ambalo si mwaminifu kwa Yesu ( Yakobo 4:4 ).
Viongozi wengi wa Matengenezo walifundisha kwamba "Babeli" wa Ufunuo 17 ni upapa.

**4. Je, tunaweza kumtambua kahaba (kanisa) anayeitwa "Babiloni Mkubwa, Mama wa Makahaba" katika Ufunuo sura ya 17?**
**Jibu:** Ndiyo, inajulikana sana kwamba kuna kanisa moja tu ambalo linadai kuwa kanisa mama, K John A. O'Brien, alisema: "Mwadhimisho huo [Utunzaji-Jumapili] unabaki kuwa ukumbusho wa Mama Kanisa ambamo madhehebu yasiyo ya Kikatoliki yalijitenga nayo. 1

**Hoja zilizotumiwa katika Ufunuo 17 kumwelezea mama Babeli na mnyama anayempanda kwa uwazi zinalingana na upapa:**

A. Aliwatesa watakatifu (mstari 6). (Ona Miongozo ya Masomo ya 15 na 20.)

B. Alikuwa amevaa nguo za zambarau na nyekundu (mstari wa 4). Mara nyingi mapapa huvaa rangi ya kifalme ya zambarau katika kazi muhimu, na nyekundu ni rangi ya mavazi ya makadinali wa Kikatoliki.

C. Vichwa saba vya mnyama (mstari wa 3) ambaye mwanamke ameketi juu yake ni milima saba (mstari wa 9). Inajulikana sana kwamba Roma, makao makuu ya ulimwengu ya upapa, imejengwa juu ya vilima saba au milima.

D. Mnyama ana hatia ya kukufuru (mstari wa 3), jambo ambalo pia linalingana kwa uwazi na upapa. (angalia Mwongozo wa 15 na 20.)

E. Alitawala "juu ya wafalme wa dunia."

Mstari wa 18. Alexander Flick anasema kwamba kufikia karne ya 13, papa alikuwa "angalau katika nadharia na kudai ... mtawala wa ulimwengu wote katika mambo ya kimwili na ya kiroho." 2 Jambo hilo halingeweza kupatana na ufalme au serikali nyingine ya kidunia. Upapa umeelezewa katika Ufunuo 17 kwa uwazi sana kwa mashaka.

**Kumbuka:** Viongozi wengi wa Matengenezo ya Kanisa ( Huss, Wycliffe, Luther, Calvin, Zwingli, Melanchthon, Cranmer, Tyndale, Latimer, Ridley, na wengineo) walifundisha kwamba upapa ndiyo mamlaka inayohusika hapa. 3

1John A. O'Brien, The Faith of Millions (Huntington, IN: Our Sunday Visitor, Inc., 1974), p. 401.

2The Rise of the Mediaeval Church (New York: Burt Franklin, 1959), pp. 575, 576.
3George Eldon Ladd, The Blessed Hope (Grand Rapids, MI: William B. Eerdman's Publishing Co., 1956), pp. 32-34.

**<u>Neno "Babeli" lilianzia Mnara wa Babeli. Ina maana "kuchanganyikiwa" au Machafuko.</u>**

**5. Ni nini maana halisi ya neno "Babiloni," na asili yake ni nini?**
"Na tujenge ... mnara, ambao kilele chake kifike mbinguni." "Bwana akasema ... na tushuke, tukaivuruge lugha yao huko, wasipate kuelewana usemi wao kwa wao." "Kwa hiyo jina lake likaitwa Babeli ["mkanganyiko", pambizo]; kwa kuwa Bwana aliichafua lugha huko." Mwanzo 11:4 , 6 , 7 , 9 .

**Jibu:** Maneno "Babeli" na "Babeli" yanamaanisha "kuchanganyikiwa." Jina la Babeli lilianzia kwenye Mnara wa Babeli, ambao ulisimamishwa baada ya Gharika na wapagani wenye ukaidi ambao walitumaini kuujenga juu sana hivi kwamba maji ya mafuriko yasingeweza kuufunika kamwe (mstari wa 4). Lakini Bwana alichanganya lugha zao, na matokeo yake machafuko yalikuwa makubwa sana wakalazimika kusitisha ujenzi. Kisha wakauita mnara huo "Babeli" (Babeli), au "mkanganyiko."

Baadaye, katika siku za Agano la Kale, ufalme wa kipagani duniani kote ulioitwa Babeli ulitokea ambao ulikuwa adui wa watu wa Mungu, Israeli. Ilitia ndani uasi, kutotii, kuteswa kwa watu wa Mungu, kiburi, na ibada ya sanamu (Yeremia 39:6 , 7 ) 50:29 , 31-33 51:24 , 34 , 47 Danieli sura ya 3 na 5). Kwa hakika, katika Isaya sura ya 14 Mungu anatumia Babeli kama ishara ya Shetani mwenyewe kwa sababu Babeli ilikuwa na uadui na uharibifu mkubwa kwa kazi ya Mungu na watu Wake. Katika kitabu cha Agano Jipya cha Ufunuo, neno "Babeli" linatumiwa kuashiria ufalme wa kidini ambao ni adui wa Israeli wa kiroho wa Mungu, kanisa Lake ( Ufunuo 14:8 ) 16:19 ).

**<u>Makanisa yanayokubali mafundisho ya uongo ya mama Babeli yanakuwa "Babeli" yenyewe.</u>**

**6. Mabinti kahaba wa Babeli mama wanaotajwa katika Ufunuo 17:5 ni akina nani?**
**Jibu:** Ni baadhi ya makanisa ambayo awali yalipinga mafundisho ya uongo ya mama Babeli na kumwacha wakati wa Matengenezo makubwa ya Kiprotestanti. Lakini, baadaye, walianza kuiga kanuni na matendo ya mama na hivyo wakaanguka wenyewe. Hakuna mwanamke anayezaliwa akiwa kahaba. Wala makanisa ambayo ni ya Kiprotestanti ambayo ni binti kwa mfano yalipozaliwa hayakuanguka. Kanisa au shirika lolote linalofundisha na kufuata mafundisho na matendo ya uongo ya Babeli linaweza kuwa kanisa au binti aliyeanguka. Kwa hiyo Babeli ni jina la familia ambalo linajumuisha kanisa mama na wale binti zake, ambao pia wameanguka.

**<u>Mnyama wa Ufunuo 17 anawakilisha serikali ya kiraia. Mwanamke akipanda juu ya mnyama ina maana kwamba kanisa linatawala serikali.</u>**

**7. Katika Ufunuo 17, kwa nini Babeli/Babiloni mama anafananishwa akiwa amempanda mnyama? Mnyama anawakilisha nini?**
**Jibu:** Katika Ufunuo 13:1-10 , Yesu anaonyesha upapa kama mchanganyiko wa kanisa na serikali. (Kwa habari zaidi, ona Mwongozo wa Kusoma 20.) Katika Ufunuo sura ya 17, Yesu anaonyesha kanisa (kahaba) na hali (mnyama) kama vyombo tofauti, ingawa vinahusiana. Mwanamke anasimama juu ya mnyama, ambayo inaashiria kwamba kanisa linatawala serikali.
Dini zisizo za Kikristo na Uprotestanti ulioasi zitajiunga na upapa kama washirika katika vita vya mwisho dhidi ya Mungu na wafuasi Wake.

**8. Ni mamlaka gani nyingine zinazoungana na upapa katika kutimiza matukio ya nyakati za mwisho?**
"Kisha nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo na kwenda kwa wafalme wa dunia na wa ulimwengu wote, kuwakusanya kwa vita vya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi." Ufunuo 16:13 , 14 .

**Jibu:** Joka la Ufunuo 12:3 , 4 na nabii wa uongo wa Ufunuo 13:11-14. 19:20 hufanya muungano na mnyama wa Ufunuo 13:1-10 , au upapa.

A. Joka la Ufunuo sura ya 12 linamwakilisha Shetani akifanya kazi kupitia Rumi ya kipagani. (Angalia Mwongozo wa Masomo 20 kwa maelezo zaidi.) Katika siku hizi za mwisho unajumuisha dini zisizo za Kikristo kama vile Ubudha, Ushinto, Uhindu, Enzi Mpya au New Age, ubinadamu wa kilimwengu au secular humanism (watu wanaosema wanaweza kuwa maadili na kujitosheleza bila kuwa na Mungu) n.k.

B. Nabii wa uongo anawakilisha Uprotestanti ulioasi uliojikita katika Amerika, ambao utaongoza katika kuhimiza na kushawishi ibada ya ulimwenguni pote ya mnyama (ona Mwongozo wa Somo 21).

C. Mnyama ni upapa (tazama Mwongozo wa Somo 20).

D. Mamlaka hizi tatu: Dini na serikali zisizo za Kikristo, Ukatoliki wa Kirumi, na Uprotestanti ulioasi zitakuwa washirika katika Har–Magedoni, vita vya mwisho dhidi ya Mungu, sheria Yake, na wafuasi Wake waaminifu. Muungano huu unaitwa "Babeli mkuu" na Yesu katika Ufunuo 18:2 .
Miujiza yenye nguvu ya Shetani na malaika zake (wanaojifanya kuwa roho za wafu) itaunganisha ulimwengu katika kumtegeza kwao mnyama.

**9. Je, mashirika yenye asili tofauti tofauti yatawezaje kuungana kwa ufanisi?**
"Hawa wana nia moja, nao watampa yule mnyama uwezo wao na nguvu zao." Ufunuo 17:13 .

**Jibu:** Ufunuo 16:13 , 14 inasema "roho wachafu kama vyura" ambao ni "roho za mashetani" watawaunganisha kupitia miujiza watakayofanya. Kuwasiliana na-roho - imani kwamba wafu wako hai na wanaweza kuwasiliana na walio hai - itakuwa kanuni ambayo itawaunganisha wote pamoja. Shetani na malaika zake, wakijifanya kuwa roho za wapendwa waliokufa watawatokea watu, manabii wa kale, malaika wa mbinguni ( 2 Wakorintho 11:13 , 14 ), na hata Kristo Mwenyewe ( Mathayo 24:24 ) watasadikisha ulimwengu kwamba kazi yao inaongozwa. kutoka mbinguni kwenyewe (ona Mwongozo wa Somo 10). Kwa bahati mbaya, vyombo vyote vitatu vinaamini kwamba wafu wako hai:

A. Ukatoliki unasali kwa Mariamu na watakatifu wengine waliokufa na unaamini kwamba watakatifu hawa huwabariki wafuasi wao kwa miujiza.

B. Dini zisizo za Kikristo karibu zote zinategemea imani na ibada ya roho za wafu. Dini za kiafrika nyingi zilisali au ziliomba baraka kwa mababa zao waliokufa 'wahenga' wakiamini wana uwezo fulani mahali fulani kuliko wao yaani kuabudu mizimu Soma kazi ya Mwanatheolojia John Mbithi na ancestors Afrika. The New Age inasisitiza "channel" inayodhaniwa kuzungumza na roho za wafu.

C. Uprotestanti ulioasi imani huamini kwamba wafu hawajafa. bali, badala yake, wako hai mbinguni au kuzimu. Hivyo wanaweza kudanganywa kirahisi na roho ovu wanaojifanya kuwa roho za wafu.

**<u>Babeli anaanguka kwa sababu anaacha Kweli ya Biblia.</u>**

**10. Mungu analaumu Babeli kwa dhambi gani?**
A. "Babeli mkuu umeanguka." Ufunuo 18:2 .
**Jibu:** Kuanguka kunamaanisha kuacha Kweli ya Biblia na ibada ya Kweli ya Mungu wa Kweli ( 2 Petro 3:17 ).

B. "Na imekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu."
Kwa uchawi wako mataifa yote yalidanganywa." Ufunuo 18:2 , 23 .
Jibu: Hapa Mungu anaishtaki Babeli kwa (1) kuwasiliana kibinafsi na mashetani kwa kuwaalika pepo wabaya katikati yake kupitia kuwasiliana na-roho, na (2) kwa kudanganya karibu ulimwengu mzima kupitia roho za uongo, za kishetani.

C. "Wakazi wa dunia wamelewa" kutokana na mvinyo ya machukizo na uasherati inayopatikana katika kikombe chake ( Ufunuo 17:2 , 4 ) 18:3 ).

**Jibu:** Neno "chukizo" katika Biblia linaashiria uwongo ( Mithali 12:22 ). Mvinyo ya Babeli, ambayo ni mafundisho ya uongo, unawasumbua na kuwatia nguvu wale wanaounywa na kuwalewesha kiroho.

D. "Wafalme wa dunia wamefanya uasherati naye." Ufunuo 18:3 .
Jibu: Kanisa ni bibi-arusi wa Kristo ( Ufunuo 19: 7 , 8 ) na lazima kumpenda na kuwa waaminifu Kwake tu, ambayo Yesu alisema inamaanisha kushika amri Zake ( Yohana 14:15 ). Upapa unalaumiwa hapa kwa kugeuka kutoka kwa mume wake,

Yesu ( Yakobo 4:4 ), na kuunda mahusiano haramu na serikali za kiraia (muungano wa kanisa na serikali) kwa ajili ya msaada wake.

E. Usafirishaji haramu wa "roho za wanadamu" ( Ufunuo 18:13 ). Jibu: Mungu hapa analaani Babeli kwa kuwatendea watu kama bidhaa badala ya kuwa wana wa thamani wa Mungu.
Kupokea mafundisho ya uwongo huleta ulevi wa kiroho, ambao hufanya kuelewa Ukweli kuwa ngumu sana.

**11. Ni baadhi ya mafundisho gani ya uwongo yaliyo katika divai ya Babeli ambayo yanawafanya watu kulewa na kuchanganyikiwa kiroho?**

**Jibu:** Cha kushangaza, baadhi ya mafundisho maarufu zaidi na yanayopendwa ya Uprotestanti leo hayapatikani katika Biblia hata kidogo. Wameleta katika makanisa ya Kiprotestanti na ;kanisa mama' la Rumi, ambao waliyapokea kutoka kwa upagani. Machache ya mafundisho haya ya uongo ni kwamba:

A. Sheria ya Mungu imerekebishwa au kufutwa.
Sheria ya Mungu haiwezi kubadilishwa au kufutwa ( Luka 16:17 ). Mwongozo wa 6 wa Utafiti unataja ushahidi usiopingika.

B. Nafsi haifi.
Biblia inataja "nafsi" na "roho" mara 1,700. Hakuna hata mara moja inazungumza kama roho isiyokufa. Watu wanakufa ( Ayubu 4:17 ), na hakuna wanaopokea kutokufa hadi ujio wa pili wa Yesu ( 1 Wakorintho 15:51-54 ). (Angalia Mwongozo wa 10 kwa habari zaidi.)

C. Wenye dhambi wanaungua milele kuzimu.
Biblia inafundisha kwamba wenye dhambi wataangamizwa kabisa (kutokuwepo), Mungu hatatoa uzima wa milelel kwa wenye dhambi, kwamba wataungua milele, la! Nafsi na mwili, zitateketea kabisa kwa moto ( Mathayo 10:28 ). Moto wa mateso wa milele haufundishwi katika Biblia. (Angalia maelezo katika Mwongozo wa 11.)

D. Ubatizo wa kuzamishwa sio lazima.
Ubatizo wa kuzamishwa ni ubatizo pekee unaotambuliwa na Maandiko. (Angalia Mwongozo wa 9 wa Somo kwa habari zaidi.)

E. Jumapili ni siku takatifu ya Mungu.
Biblia inafundisha, bila shaka, kwamba siku takatifu ya Mungu ni Sabato ya siku ya saba, Jumamosi. (Kwa maelezo zaidi, Angalia Mwongozo wa 7.)

**Kumbuka:** Mafundisho haya ya uwongo, yakiaminiwa, yanaelekea kuleta "mkanganyiko" (ambayo ndiyo neno "Babeli" linamaanisha) na kufanya kuelewa Maandiko kuwa ngumu zaidi.

**Mawazo Yenye Kufikirisha Ubongo**

Inafanya akili kufikiria kwamba huenda wengine wanakunywa divai ya Babiloni/ Babeli bila kujua. Labda hii yote ni mpya kwako. Ikiwa ndivyo, tafadhali mwombe Mungu akuongoze ( Mathayo 7:7 ). Kisha chunguza Maandiko kuona kama mambo haya ni Kweli ( Matendo 17:11 ). Ahadi ya Mungu ni kwamba utafuata pale Yesu anapokuongoza, na hatakuruhusu uishie katika makosa ( Yohana 7:17 ).
Malaika wa mbinguni watakuwa upande wa watu wa Mungu katika pigano la mwisho la dunia.

**12. Ni nani watakaokuwa upande wa Bwana katika pigano la Har–Magedoni?**

**Jibu:** Katika vita hivi vya mwisho, malaika wa mbinguni ( Waebrania 1:13 , 14 Mathayo 13:41 , 42 ) na watu wa Mungu, masalio ( Ufunuo 12:17 ) - watashirikiana na Yesu, anayeongoza majeshi ya mbinguni ( Ufunuo 19:11-16 ) dhidi ya Shetani na wafuasi wake.

Mabaki ya Mungu yanaundwa na wale wanaokataa uwongo wa Babeli (Mwongozo wa Somo 23 utatoa maelezo ya ziada). Wanajulikana kwa: (1) upendo wao kwa Yesu ( 1 Yohana 5:2 , 3 ), (2) uaminifu wao na imani katika Yeye ( Ufunuo 14:12 ), na (3) utii wao thabiti kwa Neno Lake na. amri ( Ufunuo 12:17). Yohana 8:31 , 32 ).

Katika wakati wa mwisho, Shetani atawadanganya wote ambao hawataki uthibitisho wa Maandiko wazi kwa kila fundisho la Biblia.

**13. Shetani atatumia mbinu gani katika pambano hilo la mwisho kati ya Kweli ya Mungu na uwongo wa Shetani?**
**Jibu:** Ingawa Shetani anamchukia Mungu na Mwanawe, ni mara chache sana anakiri jambo hilo waziwazi. Kwa kweli, yeye na roho waovu wake watajifanya kuwa malaika watakatifu na makasisi Wakristo waliojitolea ( 2 Wakorintho 11:13-15 ). Kile anachowasilisha kama ushahidi kwa upande wake kitaonekana kuwa cha haki, kiroho, na kama Yesu hivi kwamba karibu kila mtu duniani atadanganywa na kumfuata ( Mathayo 24:24 ). Bila shaka atatumia Biblia, kama alivyofanya alipokuwa akimjaribu Yesu nyikani ( Mathayo 4:1 , 11 ). Mantiki ya Shetani ni yenye ushawishi kiasi kwamba iliwadanganya theluthi moja ya malaika wa mbinguni, Adamu na Hawa, na (wakati wa Gharika) kila mtu alidanganywa duniani isipokuwa watu wanane.

**Neno la Mungu linafichua mbinu za Shetani.**

**14. Mkakati wa kupingana wa Mungu ni upi?**
"Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, ni kwa sababu hamna nuru ndani yao." Isaya 8:20 .

**Jibu:** Siku zote Mungu hupinga uwongo wa Shetani kwa Ukweli wa Biblia. Alipojaribiwa na Shetani nyikani, Yesu alinukuu Maandiko mara kwa mara ( Mathayo 4:1-11 ). Kupitia kwa watu Wake waliosalia, Mungu atasema Ukweli

kuhusu asili isiyo ya kibiblia ya Babeli mkuu. Ataweka wazi kwamba Babeli inawasilisha injili ya uwongo ( Wagalatia 1:8-12 ) ambayo imefungua mlango kwa mabilioni ya watu kudanganywa na kupotea. Mwenendo wa Mungu wa kupingana umeainishwa katika jumbe za malaika watatu wakuu za Ufunuo 14:6-14 , ambazo tunachunguza katika Miongozo tisa kati ya 27 ya Masomo katika mfululizo huu. Jumbe hizi tatu za ajabu zinafichua na kuonya dhidi ya uongo na udanganyifu wa Shetani na kuwaita watu kumwabudu Mungu na kumtii, si katika roho tu bali katika Kweli ya Biblia pia.

**Ujumbe wa Mungu wa wakati wa mwisho utaleta Ukweli na nuru tukufu kwa kila mtu duniani.**

**15. Je, jumbe za Mungu za wakati wa mwisho za onyo na matumaini zitakuwa na matokeo?**

"Baada ya hayo nikaona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni, mwenye uwezo mkuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake." Ufunuo 18:1 .

**Jibu:** Katika Maandiko, malaika huwakilisha wajumbe au ujumbe ( Waebrania 1:13 , 14 ). Ombi la Mungu la nyakati za mwisho linafananishwa na malaika mwenye nguvu ambaye uwezo wake ni mkuu sana hivi kwamba ulimwengu wote unaangazwa na Ukweli na utukufu wa Mungu. Ujumbe huu wa mwisho, uliotolewa na Mungu utaenda kwa wakaaji wa ulimwengu mzima ( Ufunuo 14:6 ; Marko 16:15 ; Mathayo 24:14 )

Ombi la Yesu la wakati wa mwisho litakapotolewa kwa ulimwengu wote, watu Wake wa kweli watatoka Babeli na kumfuata.

**16. Yesu atatoa wito gani wa mwisho na wa uharaka kwa wale walio Babiloni?**

**Jibu:** Atasema: "Tokeni kwake [Babeli], enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake. ." Ufunuo 18:4 , 5 .

Tafadhali Weka umakini kwamba Yesu anawataja watu wengi katika Babeli kuwa "watu Wangu". Kuna mamilioni ya Wakristo wanyoofu katika Babiloni ambao bado hawajasikia ujumbe huo wa onyo wa dharura/haraka. Watu hawa wanampenda Bwana sana, na Yesu anasema wao ni watoto Wake.

**17. Watu wa Yesu, walio katika Babiloni, wataitikiaje wasikiapo wito Wake wa kutoka?**

**Jibu:** Yesu anatoa jibu. Anasema, "Kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta, nao wataisikia sauti Yangu; "Kondoo Wangu waisikia sauti Yangu, Nami nawajua, nao wanifuata." Yohana 10:16 , 27 .

Yesu anawatambua watoto Wake walioko Babeli. Zaidi ya hayo, anaahidi kuwaita kutoka Babeli kabla haijaharibiwa. Na, jambo tukufu kuliko yote, Yesu anaahidi kwamba watu Wake ambao bado wako Babeli wataisikia na kuitambua sauti Yake na kutoka nje kwenda salama. Hivyo ni muhimu kuwahubiria watu Injili ili wafanye uamuzi ulio kamili.

**Kumbuka:** Huu ni Mwongozo wa saba wa Masomo katika mfululizo wetu wa tisa kuhusu jumbe za malaika watatu za Ufunuo 14:6-14 . Mwongozo wetu unaofuata

wa Masomo utaelezea kanisa la Mungu la wakati wa mwisho kwa uwazi sana hivi kwamba huwezi kukosa kulitambua.

**18. Ikiwa uko Babiloni sasa, je, uko tayari kutii ombi la haraka la Yesu la kutoka humo?**

**Jibu:**

**Maswali ya Kucheua**

**1. Je, kwanini nisibaki Babeli na kujaribu kumrekebisha Babeli badala ya kutoka nje?**
Hapana. Yesu anasema Babiloni itaangamizwa, si kurekebishwa. Atakuwa amelewa bila tumaini na divai yake (inayotambuliwa kama fundisho la uwongo katika Ufunuo 18:5 , 6 ). Ni kwa sababu hii ndiyo maana anawaita watu Wake watoke humo ( Ufunuo 18:4 ).

**2. Wafalme wa mashariki wa Ufunuo 16:12 ni akina nani?**
Wafalme wa mashariki ni Wafalme (Baba na Mwana) wa mbinguni. Wanaitwa wafalme wa mashariki kwa sababu huo ndio mwelekeo ambao viumbe wa mbinguni huikaribia dunia. Kumbuka yafuatayo, kwa mfano:

A. Kuja kwa Yesu mara ya pili kutakuwa kutoka mashariki ( Mathayo 24:27 ).
B. Utukufu wa Mungu unatoka mashariki ( Ezekieli 43:2 ).
C. Malaika wa Ufunuo wa kutia muhuri anatoka mashariki ( Ufunuo 7:2 ).
D. Jua, linaloashiria Yesu, linachomoza mashariki ( Malaki 4:2 ).

**3. Je, onyo kuhusu kuanguka kwa Babiloni ladokeza kwamba Babiloni hajaanguka sikuzote?**
Ndiyo inafanya kwenda kuanguka. Makanisa mengi yanayojumuisha Babeli yamekuwa yakisimama imara, yamenyooka, na kuwa na uaminifu kwa Yesu zamani. Waanzilishi walikuwa watu mashuhuri wa Mungu ambao walikuwa wakiichunguza Biblia kwa bidii ili kugundua Ukweli Wake wote. Sio makanisa yote yameanguka leo. Hata hivyo, kanisa lolote linalofundisha mafundisho ya uongo ya mama Babeli na kufuata mazoea yake linaweza kuwa mmoja wa binti zake walioanguka.

**4. Mkristo anapaswa kwenda wapi anapoitwa kutoka Babiloni?**
Tafuta watu wanaozishika amri za Mungu, na kuwa na imani ya Yesu, na wanahubiri ujumbe wa malaika watatu duniani kote, na ujiunge nao ( Ufunuo 14:6-12 ). Mwongozo wa Somo la 23 utaelezea kikamilifu kanisa la Mungu la siku za mwisho.

**5. Wafalme 10 wa Ufunuo 17:12-16 wanawakilisha nini?**
Wafalme 10 wanafananishwa na mataifa ya ulimwengu. Vidole 10 vya miguu ya sanamu ya Danieli sura ya 2 na pembe 10 za mnyama mkubwa sana wa Danieli sura ya 7 zilifananisha na falme 10 za Ulaya. Hata hivyo, maana hiyo imepanuliwa katika Ufunuo sura ya 11 hadi 18 kumaanisha “wafalme wote wa dunia” au “mataifa

yote.” (Angalia Ufunuo 16:14 ; 18:3 .)

**6. Ufananisho wa “vyura” unamaanisha nini katika Ufunuo 16:13, 14 ?**
Chura hukamata mawindo yake kwa ulimi wake, ambayo inaweza kuashiria zawadi ghushi ya ndimi ambayo inaenea ulimwenguni leo. Tafadhali kumbuka kwamba miujiza, ikiwa ni pamoja na karama ya lugha, inathibitisha jambo moja tu - nguvu isiyo ya kawaida. Lakini Biblia inatujulisha kwamba nguvu zisizo za kawaida zinaweza kutoka kwa Mungu au Shetani. Inaeleza zaidi kwamba Shetani, akijifanya kama malaika wa nuru kutoka mbinguni ( 2 Wakorintho 11:13-15 ), atatumia miujiza isiyo ya kawaida kwa ufanisi sana hivi kwamba karibu ulimwengu wote utadanganywa na kumfuata ( Ufunuo 13:3 ). Kwa sasa, anatumia kipawa ghushi cha ndimi kuunganisha makanisa na dini za kila namna – kutia ndani wapagani na waabudu roho (dini ya mizimu). Kila mmoja wa hawa anahisi kwamba karama ya ndimi ni uthibitisho wa uhalisi.

**Lazima Tuzijaribu Roho**

Biblia inaonya kwamba ni lazima tuzijaribu roho ( 1 Yohana 4:1 ). Ikiwa hazikubaliani na Biblia, basi ni bandia ( Isaya 8:19 , 20 ). Zaidi ya hayo, karama za Kweli za Roho Mtakatifu hazipewi kamwe mtu ambaye kwa makusudi na kwa kujua anamtii Mungu ( Matendo 5:32 ). Kuna karama ya Kweli ya lugha. Ni kuwezesha kimuujiza kuzungumza kwa ufasaha lugha za kigeni ambazo hapo awali hazijafunzwa na hazijulikani na mzungumzaji ( Matendo 2:4-12 ). Mungu hutumia karama hii inapohitajika kuwasilisha ujumbe Wake wa wakati wa mwisho kwa wale wa lugha nyingine. Ilihitajika siku ya Pentekoste kwa sababu vikundi vya lugha 17 vilikuwa kwenye umati na wanafunzi Wake pengine walijua lugha moja tu.

**7. Je, vuguvugu la Enzi Mpya (New Age) litachukua jukumu kubwa katika mzozo wa mwisho wa wakati wa mwisho kati ya wema na uovu?**
Bila shaka! Linahusika sana na uchawi, matukio ya kiakili, na kuwasiliana na pepo. Kuwasiliana na pepo kwa hakika kutakuwa sababu kuu katika onyesho/vituko/drama ya mwisho ya dunia. Ikiunganishwa na nguvu isiyo ya kawaida ya karama ya lugha ghushi na ikishirikiana na muungano wa makanisa ulimwenguni pote wa wakati wa mwisho, kuwasiliana na-roho kutaenea ulimwenguni pote. Imani ya Enzi Mpya (New Age) katika mawasiliano ya roho na kuzaliwa upya katika umbo lingine ni upagani wa zamani katika vazi jipya. Imani yake katika nafsi isiyoweza kufa, na isiyokufa ambayo inaweza kuwasiliana na watu wa dunia ni uwongo uleule wa kale ambao Shetani alimwambia Hawa katika Edeni: “Hakika hamtakufa.” Mwanzo 3:4 (mfano wa Age ni dini za mashariki kama Hindu huamini mtu akifa anazaliwa mahali pengine kama mfalme au mbuzi kutokana na maisha aliyoishi kabla-reincarnation) . (Ona Mwongozo wa 10 kwa maelezo zaidi kuhusu kifo.)

**8. Ni dhahiri kwamba Mungu anafunua shughuli za Mpinga Kristo au upapa katika Danieli sura ya 7 na Ufunuo sura ya 13, 17, na 18. Je, Mpinga Kristo anatajwa mahali pengine katika Maandiko?**

Ndiyo, mnyama au nguvu ya Mpinga Kristo (au shughuli zake) inarejelewa katika

angalau nabii tisa za Agano la Kale na Jipya: Danieli 7; Danieli sura ya 8, 9; Danieli 11; Ufunuo 12; Ufunuo 13; Ufunuo 16; Ufunuo 17; Ufunuo 18; na Ufunuo 19. Hakika, Mungu anapokazia nguvu zile zile mara tisa tofauti, anataka sisi tusikilize. Weka umakini katika kujisomea mwenyewe pia.

**9. Je, ufalme wa Shetani unaoitwa "Babiloni" ulianzia kwenye Mnara wa Babeli?** Hapana, ilianza wakati Shetani alipomwasi Mungu mbinguni. Kwa hakika, nabii Isaya anafananisha Lusifa wakati wa kuanguka kwake kutoka mbinguni kama mfalme wa Babeli ( Isaya 14:4 , 12-15 ). Mungu ameutazama ufalme wa Shetani kama Babeli tangu mwanzo wa dhambi. Kusudi la Shetani lililo wazi ni kumshinda Mungu, kufuta ufalme wa Mungu, na kuanzisha ufalme wake wa uasi wa Babeli ulimwenguni kote. Yesu alisema kuna pande mbili tu ( Mathayo 7:13 , 14 ). Kila nafsi duniani hatimaye itapanga mstari ama upande wa Yesu au Babeli. Ni suala la maisha na kifo. Wale wanaomtumikia na kumtegemea Yesu wataokolewa katika ufalme Wake wa mbinguni. Wale wanaounga mkono Babiloni wataangamizwa kwa moto. Na tuna wakati mdogo sana wa kufanya maamuzi. Hii ndiyo sababu kutii onyo la Yesu la wakati wa mwisho dhidi ya Babeli ni jambo muhimu sana na la haraka/dharura.

**10. Katika Ufunuo 16:12 , ni nini kinachomaanishwa na maji ya Mto Efrati kukaushwa ili kuandaa njia kwa ajili ya wafalme wa mashariki?**

Kabla ya ufalme wa kale wa Babeli kutekwa na jemadari wa Umedi Dario, maji ya mto Frati, ambayo yalipita chini ya kuta za jiji, yalielekezwa kwenye ziwa lililotengenezwa na mwanadamu au artificial lake. Ukengeushaji huo uliruhusu jeshi la Dario kuteka jiji hilo usiku kwa kuingia kutoka chini ya kuta kupitia mto usio na kitu. Katika unabii wa Ufunuo, "maji" yanafananisha watu ( Ufunuo 17:15 ). Kwa hiyo, maji ya mto Frati yanarejelea wafuasi wa "Babiloni mkuu," ambao mategemeo au matumaini yao yanakauka wanapogeuka dhidi ya Babeli kwa nia ya kumwangamiza ( Ufunuo 17:16 ) . Kukauka huku kwa uungwaji mkono kwa "Babiloni mkuu" kunawahakikishia ushindi wafalme wa mashariki, Baba wa mbinguni na Mwana.

**Maswali ya Maswali**

**1. Nini maana ya neno "Babiloni"? (1)**
_____ Kuchanganyikiwa au machafuko.
_____ Uasi.
_____ Mdanganyifu.

**2. Babiloni mama anafananishwa na nani katika unabii wa Biblia? (1)**
_____ Umoja wa Mataifa.
_____ Upapa.
_____ Maria, mama yake Yesu.

**3. Binti za mama Babeli ni akina nani? (1)**
_____ Wanawake wa Agano Jipya-Prisila, Elisabeti, na Dorkasi.
_____ Malkia wa Ulaya.
_____ Makanisa yanayofuata mafundisho na desturi potofu za mama Babeli.

**4. Ni nini kinachofananishwa na mama Babiloni anayeketi juu ya mnyama mwekundu sana? (1)**
_____ Kanisa linalodhibiti serikali, ambalo linaliunga mkono kwa karibu.
_____ Wanawake hutengeneza wakufunzi wazuri wa wanyama.
_____ Wanawake wanapaswa kupanda wanyama na sio kutembea.

**5. Ni mafundisho gani ya uwongo ya Babiloni yatachanganya watu kiroho? (4)**
_____ Utakatifu wa ndoa.
_____ Kifo ni usingizi.
_____ Wenye dhambi huungua motoni milele.
_____ Jumapili kama siku takatifu ya Mungu.
_____ Roho, au nafsi, hazifi.
_____ Ubatizo wa kuzamishwa.
_____ Sheria ya Mungu imefutwa au kurekebishwa.

**6. "Babeli umeanguka" inamaanisha kwamba (1)**
_____ Malaika alianguka kutoka mbinguni.
_____ Babeli imekumbwa na tetemeko la ardhi.
_____ Kanisa mama na makanisa mengine yanayokubali mafundisho yake ya uwongo yameanguka kutoka kwa Kweli ya Biblia na ibada ya Kweli ya Mungu wa Kweli.

**7. Ishara "Wafalme wa mashariki" inawakilisha (1)**
_____ Yesu na Baba Yake.
_____ Shetani akifanya kazi kupitia upagani.
_____ Mataifa ya ulimwengu.

**8. Kukauka kwa maji ya Mto Frati kunafananisha nini? (1)**
_____ Uhaba mkubwa wa maji katika siku za mwisho.
_____ Hakutakuwa na ugavi wa chakula katika wakati wa mwisho.

_____ Babeli itapoteza uungwaji mkono wa wafuasi wake.

**9. Babeli ni jina la familia ambalo linajumuisha karibu dini na makanisa yote. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**10. Ni nani hasa anayewaita watu kutoka Babeli? (1)**
_____ Malaika.
_____ Wafalme 10.
_____ Lusifa.
_____ Yesu.

**11. Je, haingekuwa bora kujaribu kuligeuza kanisa lililoanguka badala ya kutoka humo? (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**12. Inamaanisha nini kulewa kwa divai ya Babiloni? (1)**
_____ Kuwa mlevi.
_____ Ili kuungana naye katika karamu.
_____ Kuwa mgonjwa kimwili.
_____ Kuchanganyikiwa na mafundisho yake ya uwongo.

**13. Ni mamlaka gani tatu zitaungana kupigana dhidi ya Yesu na watu Wake katika wakati wa mwisho? (3)**
_____ Dini zisizo za Kikristo.
_____ Umoja wa Mataifa.
_____ Uprotestanti ulioasi.
_____ Wanaume wa nafasi za juu.
_____ Upapa.

**14. Yesu atakapowaita watu Wake kutoka Babeli, je, watatoka? (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**15. Watu wengi wako Babeli lakini hawajui. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**Bibi-arusi wa Kristo**

**Somo la 23**

Biblia inasema kuna mwili mmoja tu, au kanisa, ambalo Yesu anawaita watu Wake wa nyakati za mwisho - bibi-arusi wa Kristo. Kwa wengine, hili ni jambo la kuogopesha, kwa vile kuna maelfu ya makanisa mbalimbali leo ambayo yanajiita ya Kikristo. Karibu kila mmoja anadai kuwa yuko katika kanisa la Mungu, lakini kila moja linatofautiana sana katika tafsiri ya Biblia, imani, na utendaji. Haiwezekani kabisa kwa mtafutaji Ukweli mwaminifu kuchunguza madai ya kila mmoja. Hata hivyo, tunaweza kushukuru kwamba Yesu ametatua tatizo hili kwa ajili yetu kwa kuelezea kanisa Lake kwa kina hivi kwamba unaweza kulitambua kwa urahisi! Maelezo hayo, yaliyo wazi na yenye nguvu, yanapatikana katika Ufunuo 12 na 14, na yatakufurahisha kwa kweli za kushangaza ambazo zitakusaidia katika nyakati za mwisho. Tafadhali soma Ufunuo 12:1-17 kabla ya kuanza safari yako ya ugunduzi katika Kweli hizi zinazobadilisha.

**1. Yesu anawakilisha kanisa Lake la kweli kwa ishara gani ya kinabii?**
"Nimemfananisha binti Sayuni na mwanamke mzuri na mtamu." Yeremia 6:2 . "Na kuuambia Sayuni, Ninyi ni watu wangu. Isaya 51:16 .

**Jibu:** Tulijifunza katika Mwongozo wa 22 wa Somo kwamba Yesu anaashiria kanisa Lake la kweli, safi (Sayuni) kama mwanamke safi na kanisa lililoasi kama kahaba. Maandiko mengine machache ambayo pia yanatumia ishara hii ni 2 Wakorintho 11:2 Waefeso 5:22 , 23 na Ufunuo 19:7 , 8 .

**2. Katika Ufunuo 12:1, Yesu anafananisha kanisa Lake kama mwanamke "aliyevikwa jua," na "mwezi chini ya miguu yake," na amevaa "taji ya nyota kumi na mbili." Alama hizi zinamaanisha nini?**

**Jibu:** A. Jua linawakilisha Yesu, injili Yake, na haki Yake. "Bwana Mungu ni jua." Zaburi 84:11 . (Angalia pia Malaki 4:2 .) Bila Yesu hakuna wokovu ( Matendo 4:12 ). Zaidi ya kitu kingine chochote, Yesu anataka kanisa Lake lifurike na uwepo Wake na utukufu.

B. **"Mwezi chini ya miguu yake"** inawakilisha mfumo wa dhabihu wa Agano la Kale. Kama vile mwezi unavyoakisi nuru ya jua, ndivyo mfumo wa dhabihu ulivyosaidia kiroho tu kwani uliakisi mwanga kutoka kwa Masihi ajaye (Waebrania 10:1 ).

C. **"Taji ya nyota kumi na mbili "** inawakilisha kazi ya wanafunzi 12, ambayo ilitawaza miaka ya kwanza ya kanisa la Agano Jipya.

**Mtoto anayetajwa katika Ufunuo sura ya 12 ni Yesu.**

**3. Kisha, unabii unasema kwamba mwanamke yuko katika utungu, karibu kuzaa mtoto ambaye siku moja atayatawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Kisha akamzaa "mtoto mwanamume," na baadaye akachukuliwa hadi kwenye kiti cha enzi cha Mungu mbinguni ( Ufunuo 12:1, 2, 5 ). Mtoto**

**huyu alikuwa nani?**

**Jibu:** Mtoto alikuwa Yesu. Siku moja atatawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma ( Ufunuo 19:13-16 ; Zaburi 2:7-9 ). Yesu, ambaye alisulubiwa kwa ajili ya dhambi zetu, alifufuliwa kutoka kwa wafu na kupaa mbinguni ( Matendo 1:9-11 ). Nguvu Zake za ufufuo katika maisha yetu ni mojawapo ya zawadi muhimu za Yesu kwa watu Wake ( Wafilipi 3:10 ).

***Joka kuu jekundu ni Shetani,*** ambaye wakati wa kuzaliwa kwa Yesu alikuwa akifanya kazi kupitia Rumi ya kipagani.

**4. Andiko la Ufunuo 12:3, 4 latanguliza "joka kubwa jekundu" lililomchukia "mtoto mwanamume" na kujaribu kumuua wakati wa kuzaliwa. Unaweza kukumbuka joka hili kutoka kwa Mwongozo wa 20. Joka alikuwa nani?**

**Jibu:** Joka hilo linawakilisha Shetani, ambaye alitupwa kutoka mbinguni ( Ufunuo 12:7-9 ) na ambaye alikuwa akifanya kazi wakati wa kuzaliwa kwa Yesu kupitia ufalme wa kipagani wa Kirumi. Mtawala aliyejaribu kumuua Yesu alipozaliwa alikuwa Herode, mfalme chini ya Roma ya kipagani. Aliwaua watoto wote wa kiume wa Bethlehemu, akitumaini kwamba mmoja wao angekuwa Yesu ( Mathayo 2:16 ). Sehemu **ya tatu ya nyota"** inawakilisha malaika waasi ambao walitupwa kutoka mbinguni pamoja na Lusifa.

**5. Ni nini maana ya "vichwa saba" na "pembe kumi" za joka, na "theluthi moja ya nyota za mbinguni" kutupwa duniani?**

**Jibu:** A. **"Vichwa saba"** vinawakilisha vilima saba au milima ambavyo Rumi ilijengwa ( Ufunuo 17:9 , 10 ). Sasa tumekutana na mnyama mwenye vichwa saba na pembe 10 mara tatu katika Miongozo yetu ya Masomo ( Ufunuo 12:3 ) 13:1 17:3 ).

B. **"Pembe kumi"** zinawakilisha serikali, au mataifa, ambayo yanaunga mkono serikali kuu katika kuwakandamiza watu wa Mungu na kanisa. Wakati wa utawala wa Rumi ya kipagani ( Ufunuo 12:3 , 4 ), waliwakilisha makabila 10 ya washenzi waliounga mkono upapa hatimaye kuangusha ufalme wa Kirumi ( Danieli 7:23 , 24 ). Makabila haya baadaye yakawa Ulaya ya kisasa. Katika siku za mwisho, wanawakilisha mataifa yote ya ulimwengu yaliyoungana katika muungano wa wakati wa mwisho ( Ufunuo 16:14 17:12 , 13 , 16 ) ambayo itaunga mkono "Babiloni Mkubwa" katika vita vyake dhidi ya watu wa Mungu.

C. **"Theluthi moja ya nyota za mbinguni"** ni malaika
waliomuunga mkono Lusifa katika maasi yake mbinguni na waliotupwa pamoja naye ( Ufunuo 12:9 ) Luka 10:18 Isaya 14:12 ).

**<u>Mapitio na Muhtasari</u>**

**Kufikia sasa, unabii umeshughulikia mambo ya hakika ya Biblia yafuatayo:**

1. Kanisa la kweli la Mungu linatokezea, nalo linafananishwa na mwanamke safi.

2. Yesu anazaliwa katika kanisa.

3. Shetani, akifanya kazi kupitia kwa Mfalme Herode wa Rumi ya kipagani, naye anajaribu kumuua mtoto Yesu.

4. Mpango wa Shetani haufaulu.

5. Kupaa kwa Yesu kumeonyeshwa kwenye picha.
Mamilioni mengi ya watu walichomwa kwenye mti kwa sababu ya manyanyaso ya Shetani.

**6. Shetani alifanya nini baada ya kushindwa katika mpango wake wa kumwangamiza mtoto Yesu?**
"Alimtesa mwanamke aliyemzaa mtoto mwanamume." Ufunuo 12:13 .

**Jibu:** Kwa kuwa hakuweza tena kumshambulia Yesu binafsi, alilenga hasira yake na mateso kwa kanisa la Mungu na watu wake.

**<u>Mambo Sita Ya Kutambulisha</u>**

Katika Ufunuo sura ya 12 na 14, Yesu anatupa mambo sita ya maelezo ya kutumia katika kutambua kanisa Lake la nyakati za mwisho. Ziangalie unaposoma sehemu iliyobaki ya Mwongozo huu wa Utafiti.

**<u>Watu wa Mungu walikimbilia mahali pasipokuwa na watu duniani ili kuepuka mateso.</u>**

**7. Mwanamke (kanisa) lilifanya nini ili kujilinda, na "nyika" inayozungumzwa katika Ufunuo 12:6, 14 ni nini?**

**Jibu:** A. Mistari ya 6 na 14 yasema, "Yule mwanamke akakimbilia nyikani," ambako alilindwa kwa "wakati, na nyakati, na nusu wakati" (au miaka 1,260 halisi) kutokana na ghadhabu ya Shetani ambaye wakati huo alikuwa. kufanya kazi kupitia Roma ya kipapa. "Mabawa mawili" yanawakilisha ulinzi na usaidizi ambao Mungu alitoa kanisa wakati wa "jangwani" ( Kutoka 19:4). Kumbukumbu la Torati 32:11 ). Muda uliotumika nyikani ni kipindi kile kile cha miaka 1,260 cha umaarufu na mateso ya upapa (AD 538 hadi 1798) ambacho Yesu alitaja mara kwa mara katika unabii. Siku moja ya kinabii ni sawa na mwaka mmoja halisi ( Ezekieli 4:6 ).

B. Neno "jangwani" linarejelea mahali pasipokuwa na watu duniani (milima, mapango, misitu, n.k.) ambapo watu wa Mungu wangeweza kujificha kwa faragha na hivyo kuepuka maangamizi kamili ( Waebrania 11:37 , 38 ). Na walijificha, Wawaldo/waldensisi, Waalbigense, Wahuguenoti, na wengine wengi. Watu wa Mungu (kanisa Lake) wangeangamizwa kama wasingekimbia na kujificha nyikani wakati wa mateso haya mabaya ya upapa. (Katika kipindi cha miaka 40, "tangu mwanzo wa utaratibu wa Wajesuiti, katika mwaka wa 1540, hadi 1580, laki tisa waliangamizwa. Laki moja na hamsini elfu waliangamia katika Baraza la Kuhukumu Wazushi katika miaka 30." Yaani Inkwizisheni-Inquistion 1) Angalau Watu milioni 50 walikufa kwa ajili ya imani yao katika kipindi hiki cha miaka 1,260. Kanisa la Mungu halikuwepo kama shirika rasmi katika kipindi hiki cha miaka 1,260. Kuanzia AD 538 hadi 1798 lilikuwa hai lakini haikutambulika kama shirika.LiIlipotoka mafichoni baada ya ile miaka 1,260, bado lilikuwa na mafundisho na tabia zile zile kama kanisa la mitume, ambalo liliingia "jangwani" mnamo mwaka 538 BK.

**Kumbuka:** Sasa tumegundua sehemu zetu mbili za kwanza za utambulisho wa mwisho wa Yesu. Kanisa la wakati:

1. Lisingekuwepo rasmi kama shirika kati ya AD 538 na 1798.

2. Lingetokea na kufanya kazi yake ya wakati wa mwisho baada ya 1798.

Kuna Wakristo wengi wenye upendo wa ile Kweli katika makanisa ambayo yalikuwepo rasmi kabla ya 1798. Lakini hakuna hata mojawapo ya makanisa haya linaloweza kuwa kanisa la Mungu la wakati wa mwisho ambalo Yesu anawaita watu Wake wote, kwa sababu kanisa la Yesu la wakati wa mwisho lilipaswa kutokea baada ya 1798. Hii ina maana kwamba makanisa mengi maarufu ya Kiprotestanti hayawezi kuwa ya wakati wa mwisho wa Mungu. Hii ni kwa sababu yalikuwepo rasmi kabla ya 1798.

1Albert Barnes, Notes on Daniel, comment on Daniel 7:25 , p. 328.
Mabaki ya nguo ni sehemu ya mwisho iliyobaki ya kukata nguo. Kinafanana na kipande cha kwanza, yaani kipande mama.

**8. Katika Ufunuo 12:17, Mungu analiita kanisa Lake la wakati wa mwisho kuwa masalio. Neno "masalio/mabaki" linamaanisha nini?**

**Jibu: Li**namaanisha sehemu ya mwisho iliyobaki. Kwa kurejelea kanisa la Yesu, inamaanisha kanisa Lake la siku za mwisho kabisa, ambalo ni sawa kimafundisho na kanisa la mitume.
Kanisa la Mungu la masalio litazishika amri Zake na pia litakuwa na karama ya unabii.

**9. Katika Ufunuo 12:17, ni maelezo gani ya ziada ya mambo mawili ambayo Yesu alitoa kuhusu kanisa Lake la masalio la wakati wa mwisho?**

**Jibu: Li**ngeshika Amri zote Kumi, pamoja na Sabato ya siku ya saba ya amri ya nne ( Yohana 14:15). Ufunuo 22:14 ). Pia ingekuwa na "ushuhuda wa Yesu", ambao

Biblia inatuambia kuwa ni roho ya unabii ( Ufunuo 19:10 ). (Mwongozo wa Somo la 24 utatoa maelezo kamili ya karama ya unabii.)
Kwa hiyo hapa kuna mambo mawili yanayofuata ya Yesu ya utambulisho kwa ajili ya Kanisa Lake la masalio la wakati wa mwisho:

3. Litazishika amri za Mungu, pamoja na Sabato Yake ya siku ya saba ya Mungu. amri ya nne.

4. Litakuwa na karama ya unabii.

Kumbuka kwamba ingawa wengi wa Wakristo waaminifu wanapatikana katika makanisa ambayo hayashiki Sabato au kuwa na karama ya unabii, hakuna hata kanisa moja kati ya haya linaweza kuwa kanisa la Mungu la wakati wa mwisho ambalo Yesu anawaita Wakristo wote wa siku za mwisho, kwa sababu kanisa la siku za mwisho litazishika amri za Mungu na kuwa na karama ya unabii.

**Ni lazima masalio wa Mungu wawe wahubiri jumbe za malaika watatu ulimwenguni pote.**

**10. Ni mambo gani mawili ya mwisho yatakayotambulisha masalio ya Mungu ambayo kitabu cha Ufunuo chatoa?**

**Jibu:** Mambo mawili ya mwisho kati ya sita ni: (5) Litakuwa kanisa la kimishenari la ulimwenguni pote ( Ufunuo 14:6 ), na (6) Litakuwa likihubiri jumbe za malaika watatu wa Ufunuo 14:6-14 , Muhtasari au kwa kifupi soma hapa chini.

A. Hukumu ya Mungu zinaendelea. Mwabuduni Yeye! Kanisa la Mungu la nyakati za mwisho lazima liwe linahubiri kwamba hukumu ilianza mwaka wa 1844 (angalia Miongozo ya Masomo 18 na 19). Pia anawaita watu "kumwabudu Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:7 . Je, tunamwabuduje Mungu kama Muumba? Mungu aliandika jibu la swali hili katika amri ya nne. "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase." "Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya sabato akaitakasa." Kutoka 20:8 , 11 . Kwa hiyo ujumbe wa malaika wa kwanza unaamuru wote kumwabudu Mungu kama Muumba kwa kuitakasa Sabato Yake ya siku ya saba, ambayo alitupa kama ukumbusho wa Uumbaji.

B. Tokeni katika makanisa yaliyoanguka ya Babeli.

C. Usimwabudu mnyama au kupokea chapa yake, ambayo ni kufanya Jumapili kama siku takatifu. Jihadharini na ibada  bandia au feki.

Kumbuka: Hapa kuna mambo mawili ya mwisho ya utambulisho:

5. Kanisa la Mungu la wakati wa mwisho litakuwa kanisa la kimishenari duniani kote.

6. Litakuwa likihubiri na kufundisha Jumbe tatu za Ufunuo 14:6-14 .

**Sasa hebu tupitie mambo sita ambayo Yesu anatupa kwa ajili ya kulitambulisha kanisa Lake la masalio la wakati wa mwisho:**

1. Lisingekuwepo kama shirika rasmi kati ya AD 538 na 1798.

2. Lingetokea na kufanya kazi yake baada ya 1798.

3. Lingeshika Amri Kumi, ikijumuisha Sabato ya siku ya saba ya amri ya nne.

4. Lingekuwa na karama ya unabii.

5. Lingekuwa kanisa la kimishenari duniani kote.

6. Lingekuwa lifundisha na kuhubiri ujumbe wa Yesu wenye sehemu tatu kama Ufunuo 14:6-14 inavyosema.

Yesu anaahidi kwamba wale wote wanaoishi kwa dhati masharti Yake sita watalipata kanisa Lake la masalio.

**11. Sasa kwa kuwa tumeweka alama sita za utambulisho wa Yesu kwa kanisa Lake la mabaki la wakati wa mwisho, Yesu anatuambia tufanye nini, na matokeo yake yatakuwa nini?**

**Jibu:** "Tafuteni, nanyi mtapata." Mathayo 7:7 . Yesu anakupa maelezo haya sita na kusema, "Nenda ukatafute kanisa Langu." Anaahidi kwamba wale wanaotafuta vitu vya mbinguni watavipata.

**Kanisa la Waadventista Wasabato ndilo pekee linaloendana na maelezo yote sita.**

**12. Je, ni makanisa mangapi yanayolingana na maelezo haya sita?**
**Jibu:** Yesu alitoa maelezo ya kipekee na mahususi ambayo yanalingana na kanisa moja tu. Yesu hakutoa mambo ya jumla yasiyoeleweka kama vile "Kutakuwa na watu wengi wazuri katika kanisa Langu" na "Pia kutakuwa na wanafiki." Je, hizo pointi hizo mbili zihusu makanisa mangapi? Yote.

Pointi hizo mbili pia zinafaa soko la mboga na vilabu vya pombe katikati mwa jiji. Vingekuwa na vigezo vya sifa ya kila kitu hapa, na kwa hivyo hilo haimaanishi chochote. Badala yake, Yesu alitoa mambo yaliyo wazi, mahususi, yenye maelezo ya juu sana ili kwamba yalingane na kanisa moja? Wacha tuangalie vipimo mara mbili.

**Kanisa la Waadventista Wasabato:**

1. Halikuwepo kama shirika rasmi kati ya AD 538 na 1798.

2. Liliibuka baada ya 1798. Lilianza mwanzoni mwa miaka ya 1840.

3. Linazishika Amri Kumi, ikijumuisha ya nne - Sabato takatifu ya Mungu ya siku ya saba.

4. Lina karama ya unabii.

5. Ni kanisa la kimataifa la kimishenari, linalofanya kazi katika nchi 208 kati ya 236 za dunia.

6. Hufundisha na kuhubiri ujumbe mkuu wa Yesu wa mambo matatu wa Ufunuo 14:6-14 .

Yesu anakuuliza uchukue maelezo haya sita na ujiangalie mwenyewe. Ni rahisi kupima. Huwezi kukosea.

**Kumbuka:** Tafadhali kumbuka kwamba kuna Wakristo wengi wenye upendo katika makanisa yao ambayo mambo haya hayapo, lakini hakuna kanisa kama hilo linaweza kuwa mabaki ya Mungu wa nyakati za mwisho ambamo anawaita watu Wake wote kwa leo.

**13. Baada ya mmoja wa watoto wa Yesu kutii wito Wake wa onyo wenye upendo na kutoka Babiloni ( Ufunuo 18:2, 4 ), Yesu anamwomba afanye nini baadaye?**
"Ninyi mmeitwa katika mwili mmoja." Wakolosai 3:15 . "Yeye [Yesu] ndiye kichwa cha mwili, cha kanisa." Wakolosai 1:18 .

**Jibu:** Biblia inasema kwamba watu wa Mungu wameitwa katika mwili mmoja, au kanisa. Yesu anawauliza wale wanaotoka Babeli wajiunge na kanisa la masalio—ambalo Yeye Ndiye kichwa Chake. Yesu alisema, "Kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili." Yohana 10:16 . Pia anawaita "watu Wangu" katika Agano la Kale ( Isaya 58:1 ) na Agano Jipya ( Ufunuo 18:4 ). Kuhusu kondoo Wake nje ya zizi Lake (kanisa), Yeye asema, "Hao nao imenipasa kuwaleta, na sauti yangu wataisikia; kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja. "Kondoo Wangu huisikia sauti Yangu, ... nao hunifuata." Yohana 10:16 , 27 .
Mungu anapowaita watu kutoka Babeli, anawauliza wajiunge na kanisa Lake la masalio. Watu wanajiunga na kanisa Lake la masalio kwa ubatizo.

**14. Mtu huingiaje katika mwili huo, au kanisa?**
"Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi au kwamba tu Wayunani." 1 Wakorintho 12:13 .

**Jibu:** Tunaingia katika kanisa la Yesu la wakati wa mwisho la masalio kwa ubatizo. (angalia Mwongozo wa 9 wa Mafunzo kwa maelezo zaidi juu ya ubatizo.)

**15. Je, Biblia inatoa ushahidi mwingine kwamba Yesu ana kanisa moja tu la masalio ambamo anawaita watu wake wote?**

**Jibu:** Ndiyo, inafanya. Hebu tuangalie upya:

A. Biblia inasema kuna mwili mmoja tu wa Kweli, au kanisa ( Waefeso 4:4) Wakolosai 1:18 ).

B. Biblia inasema siku zetu ni kama siku za Nuhu ( Luka 17:26 , 27 ). Kulikuwa na njia ngapi za kuokoka katika siku za Nuhu? Moja tu, safina. Kwa mara nyingine tena, leo, Mungu ametoa mashua moja tu, au kanisa, ambalo itawapeleka watu Wake salama hadi ufalme Wake wa mbinguni. Hakikisha kuingia kwenye mashua sahihi! Biblia inasema, "Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." Matendo 2:47 . Ilikuwa kweli katika nyakati za mitume na bado ni kweli hadi leo.

**Mungu anaahidi kwamba kanisa lake la masalio litashinda kwa utukufu.**

**16. Ni habari gani njema kuhusu kanisa la mabaki la Mungu?**

**Jibu:**
A. Dhamira yake kuu ni "injili ya milele" ya haki kwa imani katika Yesu pekee ( Ufunuo 14:6 ).
B. Imejengwa juu ya Yesu, Mwamba ( 1 Wakorintho 3:11 ; 10:4 ), na "milango ya kuzimu haitalishinda." Mathayo 16:18 .
C. Yesu alikufa kwa ajili ya kanisa Lake ( Waefeso 5:25 ).
D. Yesu anaeleza kanisa Lake la masalio kwa uwazi sana hivi kwamba ni rahisi kulitambua. Pia anaelezea makanisa yaliyoanguka na kuwaita watu Wake kutoka huko. Shetani atawatega wale tu wanaofunga macho na mioyo yao.
E. Mafundisho Yake yote ni ya Kweli ( 1 Timotheo 3:15 ).

**17. Ni habari gani njema kuhusu masalio ya watu wa Mungu?**

**Jibu**:
A. Wataokolewa katika ufalme Wake wa mbinguni ( Ufunuo 15:2 ).
B. Watamshinda shetani kwa "nguvu" na "damu" ya Yesu ( Ufunuo 12:10 , 11 ).
C. Watakuwa na subira ( Ufunuo 14:12 ).
D. Watakuwa na imani ya Yesu ( Ufunuo 14:12 ).
E. Watapata uhuru mtukufu ( Yohana 8:31 , 32 ).

**18. Saa ya dunia imechelewa sana. Ujio wa pili wa Yesu upesi unafuatia utoaji wa jumbe za malaika watatu (Ufunuo 14:12-14). Je, ni ombi gani la dharura la Yesu sasa linahusu watu wake?**
"Ingia wewe na nyumba yako yote ndani ya safina." Mwanzo 7:1 .

**Jibu:** Katika siku za Nuhu, ni watu wanane tu (pamoja na Nuhu mwenyewe) waliotii mwaliko wa Mungu. Yesu anangoja mlangoni mwa safina Yake ya wakati wa mwisho, au kanisa la mabaki, kwa ajili yako.

**Kumbuka:** Huu ni Mwongozo wetu wa nane wa Masomo katika mfululizo wa kusisimua wa jumbe za malaika watatu za Ufunuo 14:6-14 . Mwongozo wa mwisho wa Somo la mfululizo utazungumzia karama ya unabii.

**19. Niko tayari kutii mwito wa Yesu wa kuja katika usalama wa kanisa lake la mabaki la nyakati za mwisho.**

**Jibu:**

**Maswali ya Mawazo**

**1. Uchina, yenye robo moja ya watu duniani, haijaguswa kwa haijaguswa kwa injiliimeguswa kidogo tu kwa injili** "Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyo; maana kwa Mungu yote yanawezekana." Marko 10:27 . Biblia inasema Bwana "ataimaliza kazi, na kuikata kwa haki; Warumi 9:28 . Bwana Yule Yule aliyempa Yona uwezo wa kuongoza mji mzima kwenye toba katika muda usiozidi siku 40 (Yona sura ya 3) atamaliza kazi Yake haraka sana katika siku hizi za mwisho. Anasema kazi Yake itasonga kwa kasi ya kustaajabisha hivi kwamba itakuwa karibu kutowezekana kwa kanisa la Mungu kushughulikia vya kutosha mmiminiko mwingi wa watu ( Amosi 9:13 ). Mungu aliahidi jambo hilo. Litatokea. Hivi karibuni na kwa ghafla yote yatakwisha. Kufikiri na kupanga kwa muda mrefu katika kazi ya Mungu hukosa uhakika leo. Huu ni wakati wa dharura kubwa, na dharura inadai hatua ya haraka. Wanafikra wa muda mrefu wanaweza kunaswa na kuamka wakiwa wamechelewa sana.

**2. Je, kweli kuna hatari kubwa kwamba watu wengi wanaojiita Wakristo watashikwa na shuguli na kupoteza tahadhari au kuesha na kisha kupotea wakati Yesu atakaporudi?**
Ndiyo, Yesu alionyesha jambo hilo waziwazi. Alionya kuhusu mambo kadhaa yatakayowatega na kuwaangamiza Wakristo: (1) ulafi, (2) ulevi, (3) shughuli za maisha haya, na (4) kulala usingizi ( Luka 21:34 ) Marko 13:34-36 ).

A. Ulafi ni kupitiliza kiasi katika jambo lolote - kula, kufanya kazi, kusoma, tafrija n.k. Huvuruga balansi/usawa na kuharibu fikra wazi. Pia unazuia kutumia muda na Yesu.

B. Ulevi unarejelea vitu vinavyoleta usingizi na kutupa karaha kwa mambo ya mbinguni. Mifano ni pamoja na ponografia, ngono haramu, masahaba uovu, kupuuza kusoma Biblia, kupuuza maombi, na kuepuka ibada za kanisa. Mambo kama hayo husababisha watu kuishi katika ulimwengu wa ndoto au kufikirika, usio halisi na hivyo kukosa.

C. Masumbuko ya maisha haya yanaharibu Wakristo wanaojishughulisha sana kufanya mambo mema kabisa hivi kwamba wakati wa Yesu, maombi, kujifunza Neno, kushuhudia, na kuhudhuria ibada za kanisa husongamana. Kwa kufanya hivyo, tunaondoa macho yetu kwenye lengo halisi na kuzama katika mambo ya pembeni.

D. Kulala kunamaanisha kuwa katika usingizi wa kiroho. Inaweza kuwa shida kubwa zaidi leo. Wakati mtu amelala, hajui amelala. Kuchukua uhusiano wetu na

Yesu kirahisi, kuwa na namna ya utauwa usio na nguvu, kutumia mahubiri yote makuu kwa wengine, na kukataa kujihusisha kikamilifu katika kazi ya Yesu mambo haya yote na mengine mengi huwafanya wale ambao, kama hawataamka kimiujiza; watanaswa na watalala na kuamka wakiwa wamechelewa.

**3. Nilijiunga na kanisa la Mungu la masalio na sijawahi kuwa na furaha kiasi hicho maishani mwangu. Lakini pia sijawahi kunyanyaswa sana na shetani. Kwa nini hii?**

Kwa sababu shetani huwakasirikia watu wa Mungu waliosalia na hutumia wakati wake kujaribu kuwaumiza na kuwakatisha tamaa ( Ufunuo 12:17 ). Yesu hakuahidi kwamba watu Wake hawatapata majaribu, ole, mashambulizi kutoka kwa shetani, nyakati ngumu na hata kuumizwa vibaya na Shetani. Kwa kweli, aliahidi kwamba mambo kama hayo yangewajia watu Wake ( 2 Timotheo 3:12 ). Hata hivyo, aliahidi kwa utukufu: (1) kuwapa watu Wake ushindi ( 1 Wakorintho 15:57 ), (2) kuwa pamoja na watu Wake siku zote, katika kila jambo linalowakabili ( Mathayo 28:20), (3) uwape amani ( Yohana 16:33 ; Zaburi 119:165 ), na (4) kutowaacha kamwe ( Waebrania 13:5 ). Hatimaye, Yesu na Baba Yake waliahidi kushikilia watoto Wao kwa nguvu sana kwamba hakuna mtu angeweza kuwaondoa mikononi Mwao (Yohana 10:28 , 29 ). Amina!

**4. Neno "kanisa" linamaanisha nini?**

Neno **"kanisa"** limetafsiriwa kutoka kwa neno la Kiyunani "ekklesia", ambalo **linamaanisha "walioitwa** ." Linafaa kabisa! Watu wa Yesu wanaitwa kutoka katika ulimwengu na Babeli kuingia katika zizi Lake la usalama la thamani. Watu wanakuwa sehemu ya masalio ya kanisa la Yesu la nyakati za mwisho kwa kubatizwa Yesu anapowaita. Yesu anasema, "Kondoo Wangu huisikia sauti Yangu, ... nao hunifuata." Yohana 10:27 .

**Maswali**

**1. Yesu anatumia alama gani kwa kanisa Lake la kweli katika unabii? (1)**

_____ Kwa mnara mrefu.
_____ Kama mnyama.
_____ Na malaika angavu.
_____ Kama mwanamke safi.
_____ Kwa wingu la ajabu.

**2. Je, ni "nyika" gani ambayo kanisa lilikimbilia? (1)**

_____ Mahali pa upweke kama mapango, misitu, n.k.
_____ Jangwa la Sahara.
_____ Iraq.
_____ Jangwa la Gobi.

**3. Mambo yafuatayo ni sehemu ya jumbe za malaika watatu: (3)**

_____ Babeli imeanguka. Tokeni kwake!
_____ Kuzimu huwaka milele na milele.
_____ Hukumu ya Mungu iko kwenye kikao. Mheshimu, msifu, na kumwabudu

Yeye kama Muumba kwa kushika Sabato Yake takatifu—ambayo ni ishara, au alama Yake.
_____ Mapigo yamekwisha.
_____ Kila mtu ataokolewa.
______Msimwabudu huyo mnyama wala kupokea chapa yake.

**4. Yesu anatoa alama sita za utambulisho ili kutuongoza kwa kanisa lake la masalio. Kanisa hili litakuwa (6)**
_____ Na Wakristo wengi wazuri.
_____ Wahika Amri Kumi, pamoja na Sabato.
_____ Litakuwa na  baadhi ya wanafiki.
_____ Litafurahia kuimba nyimbo kuu za Kikristo.
_____ Litaomba sana.
_____ Halikuwepo kama shirika rasmi kati ya AD 538 na 1798.
_____ Litakuwa na karama ya unabii.
_____ Litanena kwa lugha.
_____ Litakuwa kanisa la kimishenari duniani kote.
_____ Litakuwa  na majengo mengi mazuri ya kanisa.
_____ Lilisimama na kufanya  kazi yake baada ya 1798.
_____ Litahubiri na fundisha jumbe za malaika watatu za Ufunuo 14:6-14 .

**5. Kanisa lilipaswa kuwa jangwani kwa muda gani? (1)**
_____ Miaka mitano.
_____ miaka 1,000.
_____ miaka 680.
_____ miaka 1,260.
_____ miaka 33.

**6. Katika Ufunuo sura ya 12, ishara ya mtoto aliyezaliwa na mwanamke inawakilisha (1)**
_____ Kanisa la mitume.
_____ Yesu.
_____ Injili kwenda kwa Mataifa.

**7. Je, Yesu anawaita watu Wake kutoka katika ulimwengu na Babeli na kuingia katika kanisa Lake la masalio? (1)**
_____ Ndiyo.
_____   Hapana.

**8. Mtu anajiungaje na kanisa la masalio? (1)**
_____ Kwa kupeana mkono na mhubiri.
_____ Kwa kusaini kadi ya uanachama.
_____ Kwa ubatizo.
_____ Kwa kutoa mchango mkubwa.

**9. Kuna Wakristo wengi wazuri katika makanisa yote, na hata wengine ambao si washiriki wa kanisa lolote. (1)**
_____ Ndiyo.
_____  Hapana.

**10. Ni mambo gani kati ya yafuatayo yanayowafanya Wakristo washikwe na kupotea? (4)**
_____ Kuteleza.
_____ Masumbufu ya maisha haya.
_____ Kuchangamkia sana dini yako.
_____ Ulevi wa kiroho.
_____ Kulala kiroho.
_____ Kushuhudia kwa uaminifu.
_____ Kusoma gazeti.

**11. Mungu atakatisha kazi Yake duniani kwa kupeleka injili haraka kwa kila kiumbe. (1)**
_____ Ndiyo.
_____  Hapana.

**12. Ni lipi kati ya yafuatayo ambalo Mungu huwaahidi watoto Wake? (4)**
_____ Amani.
_____ Hawatakuwa na matatizo.
_____ Ushindi.
_____ Hawataugua kamwe.
_____ Hakuna awezaye kuwatoa katika mikono Yake na ya Yesu.
_____ Hatawaacha kamwe.
_____ Watakuwa matajiri.

**13. Neno "kanisa" lina maana gani kihalisi? (1)**
_____ Mahali palipopangwa ipasavyo pa kuabudia.
_____ Kusanyiko la waamini.
_____ 'Walioitwa.'
_____ Kanisa kuu.

**Je, Mungu Huwaongoza Wanajimu na Wanasaikolojia?**

**Somo la 24**

Ikiwa mtu fulani anayejiita nabii angetokea ghafula na kuanza kuvuta umati kwa jumbe zenye kusisimua, kuponya wagonjwa, kufufua wafu, kuleta moto kutoka mbinguni, na kufichua ujuzi wa siri zako za binafsi - je, ungemwamini? Je, unapaswa kuamini? Hatima yako ya mwisho inaweza kuunganishwa moja kwa moja na uwezo wako wa kutofautisha kati ya manabii wa kweli na wa uwongo. Kwa hiyo ni muhimu sana kujua Biblia inasema nini hasa kuhusu somo hili la wakati ufaao!

**1. Je, Biblia inafundisha kwamba kutakuwa na manabii wa kweli katika siku za mwisho za dunia?**
"Siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri." Matendo 2:17 .

**Jibu:** Ndiyo, wanaume na wanawake watatoa unabii katika siku za mwisho ( Yoeli 2:28-32 ).
Karama ya unabii ni muhimu kwa kulikamilisha kanisa la Mungu.

**2. Yesu katika kupaa Kwake aliweka karama ya "manabii" katika kanisa Lake, pamoja na karama nyingine nne: mitume, wainjilisti, wachungaji na walimu (Waefeso 4:7-11). Kwa nini Mungu aliweka karama hizi kanisani?**
"Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe." Waefeso 4:12 .

**Jibu:** Yesu alitoa karama zote tano kwa ajili ya kuwakamilisha watakatifu. Kukamilishwa kwa kanisa la Mungu la nyakati za mwisho hakuwezekani ikiwa mojawapo ya karama hizi tano inakosekana.
Biblia inasema kwamba Mungu anatoa zawadi ya unabii kwa wanaume na wanawake.

**3. Katika siku za Biblia, je, zawadi ya unabii ilikuwa kwa wanaume tu?**

**Jibu:** Hapana! Mbali na wanaume wengi waliokuwa na karama ya unabii, Mungu pia alitoa zawadi hiyo kwa angalau wanawake wanane: Anna ( Luka 2:36-38 ); Miriamu ( Kutoka 15:20 ); Debora ( Waamuzi 4:4 ); Hulda ( 2 Wafalme 22:14 ); na binti wanne wa Filipo, mwinjilisti ( Matendo 21:8 , 9 ).

**4. Karama hizi zilidumu kwa muda gani katika kanisa Lake?**
"Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo." Waefeso 4:13 .

**Jibu:** Hadi watu wa Mungu wote wawe Wakristo waliounganishwa, waliokomaa—ambayo, bila shaka, itakuwa hivyo mwisho wa nyakati.
Manabii hunena kama mawazo yao  yanaongozwa na Roho Mtakatifu.

**5. Manabii wa Kweli hupata habari zao kutoka chanzo gani?**
"Unabii haukuletwa kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu. 2 Petro 1:21 .

**Jibu:** Manabii wanazungumza kwa "Kuongozwa na Roho Mtakatifu." . Manabii hawaelezi maoni yao binafsi katika mambo ya kiroho. Mawazo yao yanatoka kwa Yesu, kwa njia ya Roho Mtakatifu.

**Kwa kawaida Mungu huzungumza na nabii kupitia maono na ndoto.**

**6. Mungu anazungumza na manabii kwa njia tatu tofauti. Njia hizi ni zipi?**
"Akiwapo nabii kati yenu, mimi, Bwana, nitajijulisha Kwake katika maono, Nami nitasema naye katika ndoto. "Naye nitasema mdomo kwa mdomo." Hesabu 12:6 , 8 .

**Jibu:** Maono, ndoto, au uso kwa uso.

**7. Ni nini uthibitisho wa kimwili wa nabii wa kweli katika maono?**

**Jibu:** A. Hapo anapoanza maono atapoteza nguvu za kimwili ( Danieli 10:8 ).

B. Huenda baadaye akapokea nguvu zisizo za kawaida ( Danieli 10:18 , 19 ).

C. Hawezi kupumua kabisa( Danieli 10:17 ).

D. Aweza kuzungumza ( Danieli 10:16 ).

E. Hatakuwa na ufahamu wa mazingira ya dunia (Danieli 10:5-8 2 Wakorintho 12:2-4).

F. Macho yake yatakuwa yamefunguliwa ( Hesabu 24:4 ).

**Kumbuka:** Ingawa mambo sita yaliyotangulia ya Biblia ni uthibitisho wa kimwili wa nabii wa Kweli katika maono, sio mara zote huwa hivyo. Maono ya nabii yanaweza kuwa ya kweli bila kudhihirisha ushahidi wa vipengele vyote sita.
Kufanya miujiza sio uthibitisho kwamba nabii huyu ni wa Mungu.

**8. Je, matendo ya miujiza mikuu ni uthibitisho kwamba nabii ni wa Mungu?**
"Hao ni roho za mashetani, watendao miujiza." Ufunuo 16:14 .

**Jibu:** Hapana! Ibilisi na wajumbe wake pia wana uwezo wa kufanya miujiza. Miujiza inathibitisha jambo moja tu: nguvu isiyo ya kawaida. Lakini nguvu hizo hutoka kwa Mungu na Shetani ( Kumbukumbu la Torati 13:1-5 ; Ufunuo 13:13 , 14 ).
Katika siku za mwisho, manabii wa uwongo watakuwa wenye kusadikisha sana hivi kwamba watasababisha mabilioni ya watu kudanganywa na kupotea.

**9. Yesu anatuonya kuhusu hatari gani ya wakati wa mwisho?**
"Watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule." Mathayo 24:24 .

**Jibu:** Mungu anatuonya juu ya Makristo wa uongo na manabii wa uongo ambao watakuwa na ushawishi mkubwa sana kwamba watawadanganya wote isipokuwa wateule wa Mungu. Mabilioni yatadanganywa na kupotea.
Manabii lazima wajaribiwe kwa Maandiko.

**10. Ninawezaje kujua kama nabii ni wa kweli au wa uongo?**
"Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, ni kwa sababu hamna nuru ndani yao." Isaya 8:20 .

**Jibu:** Pima mafundisho na mwenendo wao kwa Neno la Mungu, ambalo ni Biblia. Ikiwa wanafundisha na kutenda kinyume na Maandiko, wao ni manabii wa uongo na "hakuna mwanga ndani yao."
Wanasaikolojia na waaguzi wanaodai kuongozwa na roho za wafu hawaongozwi na Mungu.

**11. Je, aina fulani za manabii wa uwongo hutajwa na kushutumiwa hususani katika Biblia?**

**Jibu:** Ndiyo. Kumbukumbu la Torati 18:10-12 na Ufunuo 21:8 huzungumza dhidi ya aina zifuatazo za manabii wa uongo:

A. Mchawi - mtu anayeroga au kutumia hirizi.

B. Mtazamaji wa nyakati - mnajimu.

C. Mchawi - mtu anayedai kuwasiliana na roho za wafu.

D. Mtu anayeshauriana na mizimu - wachawi n.k.

E. Waaaguzi - watabiri au wabashiri

F. Mchawi - .

G. Necromancer - jina lingine la mchawi.

H. Mchawi - mwanamume au mwanamke anayesoma maisha ya watu.

**Kumbuka:** Wengi wa manabii hawa wa uwongo wanadai kuwa na mawasiliano na roho za wafu yaani dini ya mizimu. Biblia inasema waziwazi kwamba walio hai hawawezi kuwasiliana na wafu. (Mwongozo wa Somo la 10 una habari zaidi juu ya kifo.) Wanaofikiriwa kuwa roho za wafu ni malaika waovu, au mashetani ( Ufunuo 16:13 , 14 ). Mipira ya kioo (crystal glass, upigaji ramli), usomaji wa tende, kufafanua majani, unajimu, na kuzungumza na wanaodhaniwa kuwa ni roho za wafu si njia za Mungu za kuwasiliana na watu. Maandiko yanafundisha wazi kwamba wote wanaojihusisha na mambo hayo ni chukizo ( Kumbukumbu la Torati 18:12 ). Na mbaya zaidi, ni wale wanaoendelea kuhusika hivyo watafungiwa nje ya ufalme wa Mungu ( Wagalatia 5:19-21) Ufunuo 21:8 22:14 , 15 ).

**<u>Nabii wa Mungu atalitumikia kanisa badala ya umma kwa ujumla.</u>**

**12. Je, kazi ya nabii wa kweli kimsingi ni kutumikia kanisa au kuwahudumia wasioamini?**
"Kutoa unabii si kwa ajili ya wasioamini, bali kwa ajili yao waaminio. 1 Wakorintho 14:22 .

**Jibu:** Biblia iko wazi. Ingawa ujumbe wa nabii wakati mwingine unaweza kuadilisha umma, lengo kuu la unabii ni kulihudumia kanisa.

**13. Je, kanisa la Mungu la nyakati za mwisho lina karama ya unabii?**

**Jibu:** Katika Mwongozo wa Somo 23, tuligundua kwamba Yesu anatoa maelezo sita ya kanisa Lake la nyakati za mwisho. Hebu tupitie mambo haya sita:

A. Lisingekuwepo kama shirika rasmi kati ya AD 538 na 1798.

B. Lingetokea na kufanya kazi Yake baada ya 1798.

C. Lingeshika Amri Kumi, pamoja na Sabato ya siku ya saba ya amri ya nne.

D. Lingekuwa na karama ya unabii.

E. Lingekuwa kanisa la kimishenari duniani kote.

F. Lingehusika kufundisha na kuhubiri ujumbe wa Yesu wa mambo matatu wa Ufunuo 14:6-14 .

Ni muhimu kukumbuka kwamba kanisa la Mungu la masalio la wakati wa mwisho lazima liendane na mambo yote sita ya maelezo ya Yesu. Hii ina maana kwamba karama ya unabii lazima ijumuishwe. Kanisa la mwisho litakuwa na nabii.

**<u>Kujiunga na kanisa la Mungu, ambalo lina karama zote, kutakutia nanga kiroho.</u>**

**14. Unapojiunga na kanisa la Mungu la nyakati za mwisho, ambalo lina karama zote, Je, litakuathiri vipi?**
"ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizitumia kudanganya." Waefeso 4:14 .

**Jibu: Li**takutia nanga kiroho. Hutakuwa tena na mashaka na kutotulia katika imani yako.
Jicho la kanisa linaashiria unabii.

**15. Mtume Paulo, katika 1 Wakorintho 12:1-18, anafananisha karama ambazo Yesu alilipa kanisa na sehemu za mwili. Ni sehemu gani ya mwili**

**inayowakilisha vyema karama ya unabii?**
"Hapo zamani katika Israeli, mtu alipokwenda kuuliza swali kwa Mungu, alisema hivi, Njoo, twende kwa mwonaji; 1 Samweli 9:9 .

**Jibu:** Kwa kuwa nabii wakati mwingine huitwa mwonaji (mtu anayeweza kuona siku zijazo), macho yangewakilisha vyema zawadi ya unabii.

**<u>Kanisa lisilo na karama ya unabii ni kipofu.</u>**

**16. Kwa kuwa unabii ni macho ya kanisa, kanisa lisilo na karama ya unabii lingekuwa katika hali gani?**

**Jibu: Li**takuwa kipofu. Yesu alitaja hatari zilizofuata aliposema, "Kipofu akimwongoza kipofu, watatumbukia shimoni wote wawili. Mathayo 15:14 .

**17. Je, ni lazima kanisa la Mungu la masalio liwe na karama zote ambazo Kristo alitoa?**

**Jibu:** Ndiyo. Maandiko yanafundisha kwa uwazi kwamba kanisa la Mungu la masalio la wakati wa mwisho "halikuwa nyuma katika karama yoyote", ambayo ina maana kwamba lazima liwe na karama zote, ikiwa ni pamoja na karama ya unabii ( 1 Wakorintho 1:5-8 ) .

**18. Ufunuo 12:17 inaonyesha kwamba kanisa la Mungu la masalio ya wakati wa mwisho "litakuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo." Ufunuo 19:10 inasema kwamba "ushuhuda wa Yesu ni roho ya unabii." Je, tunaweza kuwa na uhakika kwamba hii ina maana kwamba kanisa litakuwa na nabii?**

**Jibu:** Ndiyo. Malaika alimwambia Yohana katika Ufunuo 19:10 kwamba alikuwa "mtumishi mwenzake" Yohana, mmoja wa "ndugu" zake ambao wana ushuhuda wa Yesu. Malaika huyuhuyu alirudia habari zile zile kwa Yohana katika Ufunuo 22:9 . Alisema, "Mimi ni mtumishi mwenzako, na wa ndugu zako manabii." Angalia wakati huu alijiita nabii badala ya kuwa na ushuhuda wa Yesu. Kwa hiyo, ni wazi, kuwa na "ushuhuda wa Yesu" na kuwa nabii kunamaanisha kitu kimoja.

**<u>Maneno ya nabii wa kweli ni ujumbe maalum kutoka kwa Yesu kwa watu Wake.</u>**

**19. Maneno "ushuhuda wa Yesu" yana umaana gani mwingine?**

**Jibu:** "Ushuhuda wa Yesu" unamaanisha kwamba maneno ya nabii yanatoka kwa Yesu. Kwa hiyo tunapaswa kuyachukulia Maneno ya nabii wa Kweli kama ujumbe maalum kutoka kwa Yesu kwetu ( Ufunuo 1:1). Amosi 3:7 ). Kuleta lawama, kwa vyovyote vile, juu ya nabii wa Kweli ni jambo la hatari sana. Ni sawa na kuleta suto juu ya Yesu, ambaye anawatuma na kuwaongoza. Si ajabu Mungu anaonya, "Msiwadhuru manabii Wangu." Zaburi 105:15 .

**20. Biblia ina sifa gani za kuwa nabii wa Kweli?**
**Jibu:** Vigezo vya kupima Biblia kwa nabii wa Kweli ni kama ifuatavyo:

A. Ataishi maisha ya kumcha Mungu ( Mathayo 7:15-20 ).

B. Ataitwa kumtumikia Mungu ( Isaya 6:1-10 ; Yeremia 1:5-10 ; Amosi 7:14 , 15 ).

C. Ataongea na uandike kwa kupatana na Biblia ( Isaya 8:19 , 20 ).

D. Atatabiri matukio yatakayotimia ( Kumbukumbu la Torati 18:20-22 ).

E. Atakuwa na maono ( Hesabu 12:6 ).

**21. Je, Mungu alimtuma nabii kwa kanisa Lake la masalio la nyakati za mwisho?**
**Jibu:** Ndiyo, alifanya! Haya hapa ni maelezo mafupi:

**Mungu Anamwita binti**
Kanisa la Mungu la wakati wa mwisho lilianza kuanzishwa mapema miaka ya 1840 na lilihitaji sana mwongozo. Kwa hiyo, kupatana na ahadi Yake ya Amosi 3:7 , Mungu alimwita mwanamke kijana aitwaye Ellen Harmon kuwa nabii Wake. Ellen alikubali simu. Alikuwa amejeruhiwa katika ajali akiwa na umri wa miaka tisa na ilimbidi kuacha shule akiwa na elimu rasmi ya miaka mitatu pekee, yaani darasa la tatu. Afya yake ilizorota hadi, alipoitwa na Mungu akiwa na umri wa miaka 17, alikuwa na uzito wa Kilo 32 tu na akaachiliwa afe.

**Alitumikia Miaka 70**
Ellen alikubali wito wa Mungu kwa kuelewa kwamba Yeye angemwezesha kimwili na kumfanya awe mnyenyekevu. Aliishi miaka 70 ya huduma na akafa akiwa na umri wa miaka 87. Alisisitiza kwamba leng,o na kazi yake ilikuwa kulielekeza kanisa na washiriki wake kwenye Biblia, ambayo ingepaswa kuwa kanuni yake ya imani, na zawadi ya bure ya Yesu ya uadilifu. Ellen alitimiza kila mtihani wa nabii lililotajwa katika Mwongozo huu wa Mafunzo. Hata leo Mungu anaweza kuwa na manabii wake, nasi inabidi tuwapime kwa vigezo hivi

**Jina lake, Uandishi na Vitabu**
Ellen aliolewa na James White, kasisi, na akaandika vitabu vyake chini ya jina Ellen G. White. Alikuwa mmoja wa waandishi wanawake waliofanikiwa zaidi ulimwenguni. Vitabu vyake, vinavyosomwa ulimwenguni pote, vinatoa ushauri uliovuviwa juu ya afya, elimu, kiasi, nyumba ya Kikristo, malezi, uchapishaji na uandishi, kusaidia wenye uhitaji, uwakili, uinjilisti, maisha ya Kikristo, na mengineyo.

Kitabu chake Misingi ya Elimu kinachukuliwa kuwa mamlaka katika nyanja ya elimu duniani kote. Nacho kimetumiwa na vyuo vikuu vya ulimwengu kama kitabu cha kiada, wasiliana nasi tukutumie Kopi usome. Ni kitabu chenye ujuzi muhimu kiasi kwamba kiliwahi kuibiwa na waziri wa elimu wa taifa fulani, ambaye alikichapisha kwa jina lake mwenyewe. Dk. Florence Stratemeyer, profesa wa zamani wa elimu

katika Chuo Kikuu cha Columbia, alisema kitabu hicho kina “dhana za juu za elimu” na “kilikuwa miaka hamsini mbele ya wakati wake.” Dk. Clive McCay, profesa wa zamani wa lishe katika Chuo Kikuu cha Cornell, alisema hivi kuhusu maandishi yake kuhusu afya: “Licha ya ukweli kwamba kazi za Bibi White ziliandikwa muda mrefu kabla ya ujio wa lishe ya kisasa ya kisayansi, hakuna mwongozo bora wa jumla unaopatikana leo kama kwenye vitabu vyake vya afya.” Mtangazaji wa habari Paul Harvey alisema “aliandika kwa uelewa wa kina juu ya suala la lishe hivi kwamba kanuni zote isipokuwa mbili kati ya nyingi alizounga mkono zinatumiwa kisayansi.”

Kitabu chake The Desire of Ages, juu ya maisha ya Kristo, kimepewa Jina la “kito cha Kiingereza” na Stationers Hall huko London. Inatia moyo na kuhamasiha kupitia maelezo hayo. Alisema juu ya suala la akili kwamba IQ ya mtu inaweza kuongezeka kwa muda mrefu kabla ya wataalam kukubaliana na hilo. Alisema mnamo 1905 kwamba saratani ni kijidudu (au virusi), na sayansi ya tiba ilianza kuidhinisha jambo hilo katika miaka ya 1950. Ellen G. White anasemekana kuwa mwandishi wa nne aliyetafsiriwa zaidi katika wakati wote. Kitabu chake kuhusu maisha ya Kikristo au Njia salama au kwa Kingereza Steps to Christ, kimetafsiriwa katika lugha zaidi ya 150.

Ellen White alikuwa na maono mengi, ambayo yote yanakidhi kiwango cha Biblia kwa nabii wa Kweli katika maono.

**22. Je, Ellen White alikuwa na maono?**

**Jibu:** Ndiyo, zaidi ya maono 2000. Haya yalidumu kutoka dakika chache hadi saa sita. Na yanakidhi kigezo cha Biblia cha maono kama kilivyoonyeshwa katika jibu la swali la saba la Mwongozo huu wa Kujifunza.

**23. Je, maneno ya Ellen White yamekusudiwa kuwa sehemu ya Biblia, au nyongeza ya Biblia?**

**Jibu:** Hapana! Mafundisho yanatoka katika Biblia pekee. Kama nabii wa wakati wa mwisho, lengo lake lilikuwa kusisitiza upendo wa Yesu na kurudi Kwake karibuni. Aliwahimiza watu kumtumikia na kukubali haki Yake kama zawadi ya bure. Pia alielekeza uangalifu wa watu kwenye unabii wa Biblia wa wakati wa mwisho—hasa ujumbe wa Yesu wa mambo matatu kwa ulimwengu leo ( Ufunuo 14:6-14 )—na akawahimiza washiriki ujumbe huo wa tumaini upesi na ulimwenguni pote.

**24. Je, Ellen White huzungumza kupatana na Maandiko?**

**Jibu:** Ndiyo! Maandishi yake yamejaa Maandiko. Kusudi lake lililotamkwa na lililo wazi lilikuwa kuwaelekeza watu kwenye Biblia. Maneno yake hayapingani kamwe na Neno la Mungu.

**25. Ninawezaje kumkubali Ellen White kuwa nabii wa kweli, kwa kuwa sijui alichoandika?**

**Jibu:** Huwezi, mpaka usome alichoandika. Hata hivyo, unaweza kujua kwamba yeye (1)Anakidhi vigezo vya nabii, (2) alifanya kazi ya nabii, na kwamba (3) Kanisa la Kweli la Mungu la nyakati za mwisho lazima liwe na nabii. Tunakuomba upate moja ya vitabu vyake na ukisome. (Nakala ya karatasi ya The Desire of Ages ya bei nafuu inaweza kununuliwa kutoka kwa Amazing Facts, Inc.) Unapoisoma, jiulize ikiwa inakuvuta kwa Yesu na ikiwa inapatana na Biblia. Iliandikwa kwa ajili yako. Tunadhani utapata kuvutia kabisa. Ukitaka vitabu vya Soft copy mtandaoni pia unaweza kuvipata

**26. Paulo anatupa amri gani yenye mambo matatu kuhusu nabii?**

**Jibu:** "Msidharau unabii. jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema." 1 Wathesalonike 5:20 , 21 . Mtume Paulo anasema kwamba tusimdharau au "kumpiga teke" nabii. Lakini badala yake, tunapaswa kupima kwa uangalifu kile nabii anasema na kupitia Biblia. Ikiwa maneno na tabia za nabii zinapatana na Biblia, tunapaswa kuzitii. Hivi ndivyo Yesu anauliza kwa watu Wake wa nyakati za mwisho leo.
27. Yesu anaonaje kukataliwa kwa Maneno na shauri la nabii wa kweli?
Jibu: Yesu anahesabu kukataliwa kwa nabii wa kweli kama kukataa shauri la Mungu ( Luka 7:28-30 ). Zaidi ya hayo, Anasema kwa uwazi kwamba ufanisi wa kiroho unategemea kuamini manabii Wake ( 2 Mambo ya Nyakati 20:20 ).

**Maneno ya nabii wa kweli daima huwaongoza watu kwenye funzo la kina la Biblia.**

**28. Je, manabii wa Kweli wa nyakati za mwisho huanzisha fundisho jipya, au je, mafundisho yanatoka katika Biblia tu?**

**Jibu:** Manabii wa kweli wa nyakati za mwisho hawaanzishi mafundisho mapya ( Ufunuo 22:18 , 19 ). Biblia ni chanzo cha mafundisho yote.

**Walakini, manabii wa kweli hufanya hivi:**
A. Hufichua vipengele vipya vya kusisimua vya mafundisho ya Biblia ya zamani ambavyo havikuwa dhahiri hadi ilivyoonyeshwa na nabii ( Amosi 3:7 ).

B. Huwaongoza watu wa Mungu kwenye matembezi ya karibu na Yesu na kujifunza Neno Lake kwa kina.

C. Huwasaidia watu wa Mungu waelewe sehemu ngumu, zisizoeleweka, au zisizotambulika za Biblia ili ziweze kuwa hai kwa papohapo kwa ajili yetu na kuleta furaha kubwa.

D. Husaidia kuwalinda watu wa Mungu dhidi ya ushupavu wa kidini, udanganyifu, na kuzimia kiroho.

E. Huwasaidia watu wa Mungu kuelewa unabii wa nyakati za mwisho ambao, unaothibitishwa na matukio ya habari ya kila siku, unapata maana mpya ghafla.

F. Huwasaidia watu wa Mungu kuhisi uhakika wa kurudi kwa Yesu hivi karibuni na mwisho wa dunia.

Kwa upendo unaozidi kuongezeka kwa Yesu, msisimko mpya unaotoka kwenye Biblia, na ufahamu mpya wa unabii wa Biblia, msikilize nabii wa Mungu wa wakati wa mwisho. Nawe utapata maisha yakichukua vipimo vipya vya utukufu. Kumbuka, Yesu anasema atalibariki kanisa Lake la wakati wa mwisho kwa jumbe za kinabii zenye msaada zaidi. Bwana asifiwe! Anafanya kila kitu ambacho mbingu inaweza kufikiria kwa ajili ya watu Wake wa nyakati za mwisho. Anakusudia kuwaokoa watu Wake na kuwapeleka kwenye ufalme Wake wa utukufu wa milele. Wale wanaomfuata wamehakikishiwa kuingia mbinguni ( Mathayo 19:27-29 ).

**Kumbuka:** Huu ni Mwongozo wa tisa na wa mwisho wa Somo juu ya somo la ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo 14:6-14 . Miongozo mitatu ya kuvutia ya Masomo kuhusu masomo mengine muhimu imesalia.

**29. Niko tayari kuyahakiki maandishi ya Ellen White kwa Maandiko na kuyakubali kama yanapatana na Maandiko.**

**Jibu:**

**Maswali ya Mawazo**

**1. Nini kinatokea wakati kanisa halina nabii?**
"Pasipo maono [unabii] watu huangamia; Mithali 29:18 . Wakati kanisa halina nabii wa kulishauri, kuliongoza, na kulirudisha kwa Yesu na Biblia, watu watapepesuka kwa njia ya kuchanganyikiwa ( Zaburi 74:9 ) na hatimaye kuangamia.

**2. Je, unafikiri manabii wa ziada wa kweli wanaweza kutokea kati ya leo na ujio wa pili wa Yesu?**
Kulingana na unabii wa Yoeli ( Yoeli 2:28-32 ), kwa hakika inaonekana inawezekana. Pia kutakuwa na manabii wa uongo ( Mathayo 7:15 ; 24:11 , 24 ). Ni lazima tuwe tayari kuwajaribu manabii kwa kutumia Biblia ( Isaya 8:19 , 20 ; 2 Timotheo 2:15), tukitii mashauri yao ikiwa tu ni ya kweli na kuwakataa ikiwa ni bandia. Mungu anajua wakati manabii wanahitajika ili kuwaamsha watu, kuwaonya, na kuwaelekeza kwa Yesu na Neno Lake. Alimtuma nabii (Musa) kuwaongoza watu Wake kutoka Misri ( Hosea 12:13 ). Alimtuma nabii (Yohana Mbatizaji) ili kuwatayarisha watu kwa ajili ya kuja kwa Yesu mara ya kwanza ( Mk 1:1-8 ). Pia aliahidi ujumbe wa kinabii kwa siku hizi za nyakati za mwisho. Mungu anawatuma watuelekeze kwenye Biblia na unabii Wake muhimu wa wakati wa mwisho; kututia nguvu, kutia moyo, na kutuhakikishia; na kutufanya kama Yesu ili tusiwe "bila lawama" Bwana atakaporudi. Bila msaada wa nabii, wengi watapotea kwa kurudi nyuma, kulala kiroho, na kuwa na shughuli nyingi sana. Basi tupokee jumbe za kinabii na tumsifu Mungu kwa kuzituma kwa manufaa yetu binafsi.

**3. Kwa nini makanisa mengi leo hayana karama ya unabii?**
Kwa sababu Mungu huwa anatuma manabii kwa kanisa Lake tu wakati ambapo

linashika amri Zake. Angalia jinsi Maombolezo 2:9 inavyosema: “Torati haipo tena; manabii wake nao hawapati maono kwa Bwana.” Tafadhali pitia maandiko yafuatayo: Ezekieli 7:26 ; Yeremia 26:4-6 ; Ezekieli 20:12-16 ; na Mithali 29:18 . Aya hizi zinathibitisha kwamba watu wa Mungu wanapopuuza amri Zake, Yeye hamtumi nabii. Wanapoanza kutii amri Zake, Yeye hutuma nabii kusaidia, kuhimiza, na kuongoza. Kwa hiyo wakati kanisa la Mungu la masalio la wakati wa mwisho lilipoibuka likizishika amri zake, ulikuwa ni wakati wa nabii kuinuka. Na Mungu alimtuma mmoja—pamoja kwa ratiba.

**4. Ninaweza kufanya nini ili kufanya karama ya unabii iwe na maana kwangu?** Njia ya kufanya karama ya unabii iwe na maana ni kujisomea mwenyewe na kuifuata kwa maombi ili Yesu akuongoze na kukuhifadhi na kukutayarisha kwa ajili ya kuja Kwake. “Namshukuru Mungu wangu siku zote ... kwa kuwa mmetajirishwa katika yeye katika mambo yote ... kama vile ushuhuda wa Kristo [roho ya unabii] ulivyothibitishwa ndani yenu; hata hampungukiwi katika zawadi yo yote; kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye atawathibitisha ninyi hata mwisho, mpate kuwa bila lawama katika siku ya Bwana wetu Yesu Kristo.” 1 Wakorintho 1:4-8 .

**5. Ni ipi kati ya hizi mbili--karama ya unabii au karama ya lugha---itakayochukua nafasi kubwa katika kanisa la Mungu la masalio ya nyakati za mwisho?**

Karama ya unabii itachukua jukumu kuu. Katika 1 Wakorintho 12:28 imeorodheshwa kama ya pili kwa umuhimu wa karama zote, huku karama ya kunena kwa lugha ikiorodheshwa mwisho. Kanisa lisilo na karama ya unabii ni kipofu (tazama swali la 16 katika Mwongozo huu). Yesu analionya kanisa lake la nyakati za mwisho juu ya hatari ya upofu na wan ahimiza watie macho yao dawa ya macho ya mbinguni ili waweze kuona ( Ufunuo 3:17 , 18 ). Dawa ya macho inawakilisha Roho Mtakatifu ( 1 Yohana 2:20 , 27 ; Yohana 14:26 ), ambaye hutoa karama zote kwa kanisa ( 1 Wakorintho 12:4 , 7-11 ). Kutii Maneno ya nabii wa Mungu kutasaidia masalio Wake wa mwisho kuelewa Biblia kwa uwazi na kutazuia kutokuwa na uhakika na kuchanganyikiwa.

**6. Ninaamini katika “Biblia na Biblia pekee” kama chanzo cha mafundisho na mwongozo kwa maisha ya Kikristo. Kwa hivyo, ninawakataa manabii wote wa siku hizi.**

Uko sahihi katika kuamini katika Biblia kama chanzo cha mafundisho ya Kikristo. Hata hivyo, tafadhali kumbuka kwamba Biblia inaonyesha wazi kwamba:

A. Karama ya unabii itakuwepo katika kanisa la Mungu hadi mwisho wa nyakati ( Waefeso 4:11 , 13 ).
B. Kanisa la Yesu la nyakati za mwisho litakuwa na karama ya unabii ( Ufunuo 12:17 19:10 22:9 ).
C. Kukataa ushauri wa nabii ni kukataa ushauri wa Mungu ( Luka 7:28-30 ).
D. Tumeagizwa kuwapima manabii na kufuata ushauri wao ikiwa wanazungumza na kuishi kupatana na Biblia ( 1 Wathesalonike 5:20 , 21 ).

Watu wanaoegemeza imani yao kwenye "Biblia pekee" lazima wafuate ushauri wake kuhusu manabii. Manabii wa kweli watasema sikuzote kupatana na Biblia. Manabii wanaopinga Neno la Mungu ni waongo na wanapaswa kukataliwa. Nikikosa kuwasikiliza na kuwajaribu manabii, sitegemei imani yangu juu ya Biblia, ambayo huamuru kufanya hivyo.

**Maswali**

**1. Tafadhali angalia vitu vilivyo hapa chini ambavyo vina maana sawa: (4)**
_____ Ushuhuda wa Yesu.
_____ Karama ya kunena kwa lugha.
_____ Roho ya unabii.
_____ Utabiri wa wanasaikolojia.
_____ Karama ya unabii.
_____ Kuzungumza na roho zilizokufa.
_____ Manabii wakizungumza na kanisa.

**2. Je, Mungu anatoa zawadi ya unabii kwa wanaume na wanawake? (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**3. Kulingana na Waefeso sura ya 4, ni karama gani tano ambazo Yesu aliachia kanisa wakati wa kupaa Kwake? (5 )**
_____ Manabii.
_____ Walimu.
_____ Kuimba.
_____ Kushiriki na wahitaji.
_____ Wachungaji.
_____ Mitume.
_____ Kushuhudia.
_____ Wainjilisti.

**4. Karama hizi tano, pamoja na manabii, zilidumu kwa muda gani kanisani? (1)**
_____ Mpaka tu manabii wa Agano Jipya walipokufa.
_____ Mpaka hukumu ianze.
_____ Hadi mwisho wa dunia.

**5. Kulingana na Biblia, ni mambo gani yaliyoorodheshwa hapa chini ambayo ni ya kweli kuhusu nabii katika maono? (5)**
_____ Huzungumza kwa lugha zisizojulikana.
_____ Hazungumzi kamwe wakati wa maono.
_____ Macho yabaki wazi.
_____ Mara nyingi huwa na vurugu.
_____ Havuti pumzi.
_____ Wakati fulani anaweza kusema akiwa katika maono.
_____ Hana fahamu kuhusu mazingira ya dunia.

_____ Anaweza kupokea nguvu zisizo za kawaida.

**6. Kufanya miujiza siku zote ni uthibitisho kwamba nabii ni wa Mungu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**7. Ninaweza kujua kwa hakika kwamba nabii ni wa Mungu ikiwa yeye (1)**
_____ ni mpole na mwenye neema katika mwenendo.
_____ Hufanya miujiza ya ajabu.
_____ Anang'aa sana.
_____ Anaonekana kuijua Biblia vizuri.
_____ Anafanana na Yesu.
_____ Anazungumza na kutenda kupatana na Biblia.

**8. Ni lipi kati ya yafuatayo ambalo halijashutumiwa na Biblia? (1)**
_____ Mtabiri.
_____ Wanasaikolojia wa kiume na wa kike.
_____ Mnajimu.
_____ Mchawi.
_____ Mtu anayeroga au kutumia hirizi.
_____ Msomaji mikono au mpiga ramli.
_____ Nabii anayezungumza na kuishi kupatana na Biblia.

**9. Kazi kuu ya nabii ni kutumikia kanisa. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**10. Kanisa haliwezi kuwa kanisa la kweli la Mungu la nyakati za mwisho isipokuwa liwe na nabii. (1)**
_____ Kweli.
_____ Uongo.

**11. Ni sehemu gani ya mwili inayowakilisha unabii? (1** )
_____ Mdomo.
_____ Mikono.
_____ Miguu.
_____ Masikio.
_____ Macho.

**12. Manabii wa ziada wa kweli wa nyakati za mwisho wanaweza kutokea kabla ya ujio wa pili wa Yesu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**13. Kufuata "Biblia na Biblia pekee" ina maana kwamba mtu lazima amkubali nabii wa kweli. (1)**
_____ Ndiyo.

_____ Hapana.

**14. Ni mambo gani matatu kuhusu unabii ambayo Biblia inaamuru katika 1 Wathesalonike 5:20, 21 ? (3)**
_____ Msiwadharau manabii au unabii.
_____ Fuata manabii wote.
_____ Thibitisha au jaribu maneno na matendo ya nabii kupitia Biblia.
_____ Waulize manabii kama ni wa kweli au wa uongo.
_____ Amini, au shikilia sana lililo jema.
_____ Wapuuze manabii wote.

**15. Tunapokataa ushauri wa nabii wa kweli, tunakataa ushauri wa Mungu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**16. Manabii wa kweli wa nyakati za mwisho hufundisha mafundisho mapya ambayo hayapatikani katika Biblia. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**17. Kwa nini makanisa mengi hayana nabii au manabii wa kweli? (1)**
_____ Hawangewaamini kama wangekuja.
_____ Hawashiki amri zote za Mungu.
_____ Wana mwanga wote wanaohitaji bila nabii.

**18. Pasipo maono, watu huangamia. (1)**
_____ Kweli.
_____ Uongo.

**19. Kanisa lisilo na karama ya unabii ni kipofu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

## Tunamtumaini Mungu?

## Somo la 25

Unamwamini Mungu... kweli? Ukweli ni kwamba, watu wengi wanaweza kusema ndiyo, lakini hawafanyi hivyo. Na mbaya zaidi, kwa sababu hawamwamini, wanaweza kumuibia! “hebu eleza!” unasema, “Hakuna mtu angeweza kuiba au kunyakua pesa kutoka kwa Mungu.” Lakini ujumbe wa Mungu wenye kushtua kwa watu Wake ni, “Ninyi mmeniibia” ( Malaki 3:8 ). Rekodi za Kweli zinathibitisha kwamba mabilioni ya watu humwibia Mungu, na ingawa inaweza kuonekana kuwa ya kushangaza, wanatumia pesa hizo zilizoibwa ili kwa maslah yao ya kizembe! Hata hivyo wengi hawajui ufujaji wao, na katika Mwongozo huu wa Somo, tutakuonyesha jinsi ya kuepuka kosa lile lile na jinsi ya kufanikiwa kifedha kupitia imani ya Kweli

kwa Mungu.

Sehemu ya kumi ya mapato ya mtu ni ya Mungu.
**1. Kulingana na Biblia, ni sehemu gani ya mapato yetu ni ya Bwana?**
"Na zaka yote ya nchi ... ni ya Bwana." Mambo ya Walawi 27:30 .

**Jibu:** Zaka ni ya Mungu.
Neno "zaka" maana yake halisi ni "kumi."

**2. "zaka" ni nini?**
"Nimewapa wana wa Lawi sehemu yote ya kumi katika Israeli kuwa urithi wao. "Zaka ya wana wa Israeli ... nimewapa Walawi kuwa urithi wao." Hesabu 18:21 , 24 .

**Jibu:** Zaka ni moja ya kumi ya mapato ya mtu. Neno "zaka" maana yake halisi ni "kumi." Zaka ni ya Mungu. Hiyo Ni Yake. Sina haki ya kuiweka kibindoni. Ninapotoa zaka, sitoi zawadi; Ninamrudishia Mungu kile ambacho tayari ni Chake. Nisipotoa asilimia kumi ya mapato yangu, mimi, sitoi zaka.
Zaka inapaswa kuletwa katika ghala la Mungu, au kanisa.

**3. Ni wapi Bwana anawauliza watu Wake kuleta zaka?**
"Leteni zaka zote ghalani. Malaki 3:10 .
**Jibu:** Anatutaka tulete zaka kwenye ghala Yake.

**4. Bwana anarejelea nini anapozungumza kuhusu ghala Yake?**
"Ndipo Yuda wote wakaleta zaka ya nafaka, na divai mpya, na mafuta, kwenye hazina." Nehemia 13:12 . (Rejea ya pambizoni inaita hazina "maghala.")
**Jibu:** Katika Malaki 3:10 , Mungu anaitaja ghala kama "nyumba Yangu," ambayo ina maana ya hekalu Lake au kanisa. Nehemia 13:12 huonyesha zaidi kwamba zaka yapaswa kuletwa kwenye hazina ya hekalu, ambayo ni ghala la Mungu. Maandiko mengine yanayorejelea ghala kuwa hazina za hekalu, au vyumba, angalia ndani ya 1 Mambo ya Nyakati 9:26 (angalia mafungu ya pambizo pia); 2 Mambo ya Nyakati 31:11 , 12 (angalia pambizo); na Nehemia 10:37 , 38 . Katika nyakati za Agano la Kale, watu wa Mungu walileta asilimia 10 ya maongezeko yao yote—pamoja na mazao na wanyama—kwenye ghala.

**5. Wengine wamefikiri kwamba kutoa zaka ilikuwa sehemu ya utaratibu wa Musa wa maadhimisho au sherehe ambazo ziliishia msalabani (ceremonial laws). Je, Biblia inatusaidiaje kuelewa kwamba sivyo?**
"Naye [Abramu] akampa zaka ya vitu vyote." Mwanzo 14:20 . Na katika Mwanzo 28:22 , Yakobo akasema, "Na katika kila utakalonipa hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi."

**Jibu:** Vifungu hivi vinafunua kwamba Ibrahimu na Yakobo, walioishi muda mrefu kabla ya siku za Musa, walitoa zaka ya mapato yao. Kwa hiyo tunaweza kuhitimisha kwamba mpango wa Mungu wa kutoa zaka ulitangulia sheria ya Musa.
Yesu aliwaeleza Mafarisayo kwamba ingawa walipaswa kutoa zaka, hawakupaswa

kupuuza mambo muhimu zaidi ya haki, rehema, na uaminifu.

**6. Lakini je, Yesu hakubatilisha mpango wa kutoa zaka?**
"Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! …wala yale mengine msiyaache.." Mathayo 23:23 .

**Jibu:** Hapana! Kinyume chake, Aliidhinisha. Yesu alikuwa akiwakemea Wayahudi kwa kuacha mambo muhimu zaidi ya sheria--"hukumu, rehema, na imani"--hata kama walitoa zaka kwa uangalifu sana. Kisha aliwaambia wazi kwamba wanapaswa kuendelea kutoa zaka, lakini pia wanapaswa kuwa waadilifu na wenye huruma na waaminifu.
Katika siku za Agano la Kale, zaka ilitumika kuwalipa makuhani.

**7. Zaka ilitumika kwa nini katika siku za Agano la Kale?**
"Nimewapa wana wa Lawi sehemu yote ya kumi katika Israeli kuwa urithi wao, kwa ajili ya utumishi wao wautumikiao, maana, ni utumishi wa hema ya kukutania." Hesabu 18:21 .

**Jibu:** Zaka katika siku za Agano la Kale ilitumika kwa mapato ya makuhani. Kabila la Lawi (makuhani) halikupokea sehemu ya ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo na biashara, huku yale makabila mengine 11 yalipokea. Walawi walifanya kazi ya wakati wote wakitunza hekalu na kuhudumia watu wa Mungu. Kwa hiyo mpango wa Mungu ulikuwa kwamba zaka iwasaidie makuhani na familia zao.
Leo, zaka yapaswa kutumika kulipa mishahara ya watumishi wa Mungu.

**8. Je, Mungu alibadilisha mpango Wake wa matumizi ya zaka katika siku za Agano Jipya?**
"Hamjui ya kuwa wale wahudumuo katika vitu vitakatifu huishi katika mambo ya hekalu, na hao waitumikiao madhabahu hushiriki madhabahu? Vivyo hivyo Bwana ameagiza waihubirio Injili wapate kuishi kwa ajili ya Injili; ." 1 Wakorintho 9:13 , 14 .

**Jibu:** Hapana! Ameendelea. Mpango Wake leo ili kwamba zaka itumike kusaidia wale wanaofanya kazi pekee katika huduma ya injili. Ikiwa watu wote walitoa zaka na zaka basi zingetumika kikamilifu kwa ajili ya msaada wa watenda kazi wa injili, kungekuwa na zaidi ya fedha za kutosha kufikia dunia nzima haraka sana na ujumbe wa injili wa Mungu wa wakati wa mwisho.
Mungu anaahidi kwamba warudishaji wa zaka waaminifu watapata baraka kubwa sana kwamba hawatakuwa na nafasi ya kutosha kuzipokea.

**9. Ni pendekezo gani la kustaajabisha ambalo Mungu hutoa kwa watu wanaohisi kutokuwa na uhakika kuhusu kutoa zaka?**
"Leteni zaka zote ghalani, mkanijaribu kwa hayo, asema Bwana wa majeshi, kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagia baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha. kupokea." Malaki 3:10 .
**Jibu:** Anasema, "Nithibitishe sasa" na uone kama "sitakumiminia baraka" wazo kubwa sana kupokea. Huu ndio wakati pekee katika Biblia ambapo Mungu hutoa

pendekezo kama hilo. Anasema, “Mjaribu. Atafanya kazi. Anakuahidi.” Malaki ya watoa zaka ulimwenguni pote watashuhudia kwa furaha Ukweli wa ahadi ya zaka ya Mungu. Wote wamejifunza Ukweli wa maneno haya: “Huwezi kutoa au kuariki kumshinda Mungu.”

**10. Tunapotoa zaka, ni nani hasa anapokea pesa zetu?**
“Na hapa watu wanaokufa hupokea sehemu ya kumi; Waebrania 7:8 .

**Jibu:** Yesu, Kuhani wetu Mkuu wa mbinguni, anapokea zaka zetu.
Ninapochukua zaka ya Mungu na kuitumia kwa ajili yangu mwenyewe, narudia dhambi ya Adamu na Hawa.

**11. Ni jaribu gani ambalo Adamu na Hawa walishindwa, ambalo sote lazima tulipitie ikiwa tungerithi ufalme Wake wa mbinguni?**

**Jibu:** Walichukua vitu ambavyo Mungu alisema si vyao. Mungu aliwapa Adamu na Hawa matunda ya miti yote katika bustani ya Edeni isipokuwa mti mmoja wa ujuzi wa mema na mabaya ( Mwanzo 2:16 , 17 ). Matunda ya mti huo hayakuwa yao kula. Walipaswa kuuacha kabisa. Hawa alisema hawakupaswa hata kuugusa ( Mwanzo 3:3 ). Lakini hawakumwamini Mungu. Walikula tunda na kuanguka dhambi - na Mfarakano mrefu, wa kutisha, wa kuumiza katika dhambi ulianza. Kwa watu leo, Mungu huwapa utajiri, hekima, na mali nyingine zote na baraka za mbinguni.

Kila kitu ni chetu - isipokuwa moja ya kumi ya mapato yetu, ambayo ni Yake ( Mambo ya Walawi 27:30 ). Lakini kama ilivyokuwa kwa Adamu na Hawa, Yeye haichukui kwa nguvu. Anaiacha ndani ya uwezo wetu lakini anaonya, “Usiichukue. Ni takatifu. Ni Yangu.” Yeye amekupa uchaguzi. Tunapochukua zaka ya Mungu kimakusudi na kuiweka sawa kwa matumizi yetu wenyewe, tunarudia dhambi ya Adamu na Hawa na hivyo kuonyesha ukosefu wa kuhuzunisha wa kumwamini Mkombozi wetu. Mungu hahitaji pesa zetu, lakini anastahili uaminifu na uaminifu wetu.

**<u>Mfanye Mungu kuwa Mshirika Wako</u>**

Ninapomrudishia Mungu zaka, ninamfanya kuwa mshirika katika kila jambo ninalofanya. Ni fursa nzuri sana, iliyobarikiwa kama nini: Mungu na mimi - washirika, yaani tuna Ubia! Pamoja Naye kama mshirika wangu, nina kila kitu cha kupata na hakuna cha kupoteza. Ni jambo la hatari sana kuchukua pesa za Mungu Mwenyewe, ambazo ameziweka kwa ajili ya kuokoa roho za watu, na kuzitumia kwa bajeti zetu binafsi. Ni Kupora (robbing)

Watu wa Mungu hutoa matoleo kwa furaha kama wonyesho wa upendo wao Kwake.

**12. Mbali na zaka, ambayo ni ya Mungu, ni nini kingine ambacho Mungu anaomba kwa watu Wake?**

“Leteni sadaka, mkaingie nyuani mwake.” Zaburi 96:8 .
**Jibu:** Bwana anatuomba tutoe matoleo kwa ajili ya kazi Yake kama onyesho la

upendo wetu Kwake na shukrani zetu kwa baraka Zake.
Biblia haitaji kiasi kinachopaswa kutolewa kwa ajili ya matoleo.

**13. Nitampa Mungu kiasi gani kama matoleo?**

"Kila mtu na atoe kama alivyokusudia moyoni mwake; si kwa huzuni wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa ukunjufu." 2 Wakorintho 9:7 .

**Jibu:** Biblia haitaji kiasi maalum cha matoleo. Kila mtu anaamua (kama Mungu anavyomvutia) ni kiasi gani cha kutoa na kisha kutoa kwa furaha.

**14. Ni kanuni gani za ziada za Biblia ambazo Mungu anashiriki nasi kuhusu kutoa?**

**Jibu:** A. Kipaumbele changu cha kwanza kiwe kujitoa kwa Bwana, kutoa moyo wangu ( 2 Wakorintho 8:5 ).

B. Ninapaswa kumpa Mungu kilicho bora kabisa ( Mithali 3:9 ).

C. Mungu hubariki atoaye kwa ukarimu ( Mithali 11:24 , 25 ).

D. Ni heri kutoa kuliko kupokea ( Matendo 20:35 ).

E. Ninapokuwa bahili, situmii baraka nilizopewa na Mungu ipasavyo ( Luka 12:16-21 ).

F. Mungu anarudisha zaidi ya nitoavyo mimi ( Luka 6:38 ).

G. Ninapaswa kutoa kulingana na jinsi ambayo Mungu amenifanikisha na kunibariki ( 1 Wakorintho 16:2 ).

H. Nitoe kadiri niwezavyo ( Kumbukumbu la Torati 16:17 ).

Tunarudisha zaka kwa Mungu, ambaye tayari ni mali hiy ni mali Yake. Tunatoa sadaka. Sadaka ni ya hiari na inapaswa kutolewa kwa furaha.
Dunia na vyote vilivyomo ni mali ya Mungu.

**15. Bwana anamiliki nini?**

**Jibu:**
A. Fedha na dhahabu zote duniani ( Hagai 2:8 ).

B. Dunia na watu wake wote ( Zaburi 24:1 ).
C. Bwana anamiliki dunia na vyote vilivyomo ( Zaburi 50:10-12 ). Lakini anawaruhusu watu kutumia utajiri Wake mkuu. Pia huwapa hekima na uwezo wa kufanikiwa na kujikusanyia mali ( Kumbukumbu la Torati 8:18 ). Kwa malipo ya kuandaa kila kitu, Mungu anachoomba tu ni kwamba tumrudie Yeye asilimia 10

kama utambuzi wetu wa uwekezaji Wake mkubwa katika mambo yetu ya biashara, pamoja na matoleo kama onyesho la upendo na shukrani zetu.
Mungu huwaona watu wasiootoa kuwa ni wanyang'anyi yaani wale ambao hawatoi zaka na kutoa sadaka.

**16. Je, Bwana anawatajaje watu ambao hawarudishi asilimia 10 Yake na kutoa sadaka?**
"Je! Mtu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mmeniibia Mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa jinsi gani? Katika zaka na dhabihu." Malaki 3:8 .

**Jibu:** Anawataja kuwa ni majambazi. Je, unaweza kufikiri mtu anayemwibia Mungu? Wale wanaomwibia Mungu kwa kumnyima zaka na matoleo hawataruhusiwa kuingia mbinguni.

**17. Mungu anasema nini kitatokea kwa wale ambao kwa kujua wanaendelea kumwibia zaka na matoleo?**
"Ninyi mmelaaniwa kwa laana; kwa maana mmeniibia Mimi, naam, taifa hili zima." Malaki 3:9 . "Wala wevi, wala wachoyo, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi hawataurithi ufalme wa Mungu." 1 Wakorintho 6:10 .

**Jibu:** Laana ya Mungu itakuwa juu yao. Hawataurithi ufalme wa mbinguni.
Kujishughulisha na kukusanya pesa kunamfanya mtu azishike na kujivunia nazo.

**18. Mungu anatuonya dhidi ya tamaa. Kwa nini ni hatari sana?**
"Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako." Luka 12:34 .

**Jibu:** Kwa sababu mioyo yetu inafuata uwekezaji wetu. Ikiwa lengo langu ni kukusanya pesa zaidi na zaidi, moyo wangu unakuwa wa kutamani, kubania, na kiburi. Lakini ikiwa lengo langu ni kushiriki na kuwasaidia wengine na kubariki kazi ya Mungu, basi moyo wangu unakuwa wa kujali, wenye upendo, mkarimu/huria, na mnyenyekevu. Tamaa ni mojawapo ya dhambi 20 za kutisha za siku za mwisho ambazo zitawafunga watu kutoka mbinguni ( 2 Timotheo 3:1-7 ).
Kumwibia Yesu humhuzunisha sana.

**19. Yesu anahisije tunapomnyang'anya zaka Yake takatifu na matoleo ya upendo?**
"Kwa hiyo nalihuzunishwa na kizazi kile, nikasema, Siku zote wamepotoka mioyoni mwao." Waebrania 3:10 .

**Jibu:** Pengine anahisi kama mzazi ambaye mtoto wake anamwibia pesa. Pesa yenyewe, sio kitu kikubwa. Ila ule ukosefu wa uadilifu, upendo, na uaminifu wa mtoto ndio ambao unakatisha tamaa sana.
Upendo uliwafanya watu wa Mungu huko Makedonia watoe kwa ukarimu sana kwa Wakristo waliokumbwa na njaa huko Yerusalemu.

**20. Ni mambo gani yenye kusisimua ambayo Paulo anakazia kuhusu usimamizi-nyumba wa waamini katika Makedonia?**

**Jibu:** Paulo alikuwa ameyaandikia makanisa ya Makedonia kuwaomba tafadhali watenge pesa kwa ajili ya watu wa Mungu huko Yerusalemu, ambao walikuwa wakiteseka sana kutokana na njaa iliyoendelea. Aliwaambia angechukua zawadi hizi atakapokuja katika miji yao kwenye ziara yake inayofuata. Jibu la kusisimua kutoka kwa makanisa ya Makedonia, linalofafanuliwa katika 2 Wakorintho sura ya 8, ni la kutia moyo sana:

A. Mstari wa 5A ni hatua ya kwanza, waliweka wakfu upya maisha yao kwa Yesu Kristo.

B. Mistari ya 2, 3 Ingawa walikuwa katika "umaskini mwingi" wenyewe, walitoa "zaidi ya uwezo wao" kutoa.

C. Mst 4 Walimsihi Paulo aje kuchukua zawadi zao.

D. Mstari wa 9 Karama zao zilifuata mfano wa dhabihu wa Yesu.

**Kumbuka:** Ikiwa tunampenda Yesu kweli, kutoa kwa kujidhabihu kwa ajili ya kazi Yake hakutakuwa mzigo kamwe, lakini badala yake ni fursa tukufu ambayo tutafanya kwa furaha na kuridhika sana.
Mtu anapotoa fungu la kumi, Mungu hunyoosha sehemu iliyobaki yaani tisa ya kumi iliyobaki ili iwe ya kutosha kila wakati.

**21. Mungu anaahidi kufanya nini kwa wale walio waaminifu katika kurudisha zaka na kutoa matoleo?**
"Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa hayo, asema Bwana wa majeshi, ikiwa sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hapatakuwa na nafasi ya kutosha ya kuupokea. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu, wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika shamba, asema Bwana wa majeshi. . Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi." Malaki 3:10-12 .

**Jibu:** Mungu anaahidi kuwafanikisha mawakili Wake waaminifu kifedha, na watakuwa baraka kwa wale walio karibu nao.

**<u>Fikiria Njia Zifuatazo Mungu Anazobariki:</u>**

A. Mungu anaahidi kwamba sehemu yako iliyobaki yaani 9/10 itaenda mbali zaidi na baraka Zake kuliko mapato yako yote bila hiyo. Ikiwa una shakana hili, mwulize mtoa zaka yoyote mwaminifu.

B. Baraka si lazima ziwe za kifedha mara zote. Huenda zikaletea mwili afya, amani ya akili, sala zilizojibiwa, ulinzi, familia iliyoshikamana na yenye upendo, nguvu za kimwili zilizoongezwa, uwezo wa kufanya maamuzi ya hekima, roho ya shukrani, uhusiano wa karibu zaidi pamoja na Yesu, kufaulu katika kupata nafsi, na gari la zamani linaloendelea kufanya kazi kwa muda mrefu, nk.

C. Mungu anakuwa mshirika wako katika kila kitu. Hakuna mtu isipokuwa Mungu Ndiye Ambaye angeweza kuunda mpango wa ajabu kabisa kama huu.

**22. Je, uko tayari kuanza kutoa zaka ya mapato yako na kutoa matoleo ili kuonyesha upendo wako na shukrani?**
**Jibu:**

**Maswali ya Mawazo**

**1. Sitoi zaka kwa sababu sipendi jinsi kanisa langu linavyotumia pesa za Mungu.** Zaka ni amri ya Mungu. Zaka ni fedha takatifu ambayo ni mali ya Bwana ( Mambo ya Walawi 27:30 ). Unapotoa zaka, unamtolea Yeye zaka. Mungu ni mkuu vya kutosha kutunza pesa unazotoa kwa ajili ya kanisa lake. Wajibu wako ni kutoa zaka. Mwachie Mungu awashughulikie wale wanaotumia fedha zake vibaya. Mjane wa senti mbili alipotoa fedha alipongezwa japo Yesu alijua mafarisayo ni wezi, hakusema, mama acha usitoe kuna matapeli humu, bali alimpongeza sana!

**2. Nimechanganyikiwa kwa sababu matatizo ya kifedha yamenifanya nishindwe kutoa sadaka zaidi ya zaka yangu. Ninahisi hatia kwani injili ina makubwa.** Ukubwa wa zawadi yako sio muhimu ikiwa unafanya bora uwezavyo. Yesu alisema kwamba mjane maskini wa Marko 12:41-44 , ambaye alitoa kidogo tu (senti mbili za fedha), alitoa zaidi "kuliko wote waliotia katika sanduku la hazina" kwa sababu wale wengine walitoa "katika wingi wao; lakini yeye .. alitoa vyote alivyokuwa navyo." Bwana hupima karama zetu kwa kiasi cha dhabihu tunayotoa na kwa mtazamo au roho tunayotoa. Yesu anahesabu karama yako kuwa kubwa sana. Itoe kwa furaha na ujue kwamba Yesu amependezwa. Soma 2 Wakorintho 8:12 ili upate kutia moyo.

**3. Je, uwakili hauhusishi zaidi ya utunzaji sahihi wa pesa zangu?** Ndiyo, uwakili unahusisha utunzaji unaofaa wa kila talanta na baraka ninazopokea kutoka kwa Mungu, ambaye hunipa kila kitu ( Matendo 17:24 , 25 ). Kwa kweli, inahusisha maisha yangu!

**<u>Uwakili mwaminifu wa karama za Mungu kwangu pia unajumuisha muda wangu uliotumika:</u>**

A. Kufanya kazi ambayo Mungu amenikabidhi ( Marko 13:34 ).

B. Kumshuhudia Kristo kikamilifu ( Matendo 1:8 ).

C. Kusoma Maandiko ( 2 Timotheo 2:15 ).

D. Kuomba ( 1 Wathesalonike 5:17 ).

E. Kuwasaidia wenye uhitaji ( Mathayo 25:31-46 ).

F. Kila siku kusalimisha maisha yangu upya kwa Yesu ( Warumi 12:1 , 2 ; 1

Wakorintho 15:31 ).

**4. Je, huoni kwamba wahubiri wengine wanalipwa pesa nyingi sana?**

Ndiyo, bila shaka. Kujisifu kwa utajiri kwa baadhi ya makasisi leo kunapunguza ushawishi wa wahudumu wote. Kunaleta aibu kwa jina la Yesu. Inasababisha mamia ya maelfu kurudi nyuma kwa kuchukizwa na kanisa na huduma Yake. Viongozi wa aina hiyo watakabiliwa na siku mbaya ya hesabu katika hukumu. Ila hayo yanawahusu wao na si sisi. Kama unaweza kuripoti mahali kuhusu shida ya ubaradhifu kanisani, fanya hivyo.

**Wahudumu wa Kanisa la Mungu la Masalio la Wakati wa Mwisho**

Hata hivyo, hakuna mhudumu ambaye analipwa pesa zote zilizosalia katika kanisa masalio. Baada ya mafunzo kazini, wahudumu wote hupokea takriban mshahara sawa (unaotofautiana dola chache tu kila mwezi) bila kujali cheo chao cha kazi au ukubwa wa kanisa lao. Mara nyingi, wanandoa au mke hufanya kazi katika sekata za umma ili kuongeza mapato ya wachungaji.

**5. Je, ikiwa sina uwezo wa kulipa zaka?**

Mungu anasema tukimtanguliza, atahakikisha kwamba mahitaji yetu yote yanatimizwa ( Mathayo 6:33 ). Hisabati Yake mara nyingi hufanya kazi kinyume kabisa na dhana ya mwanadamu. Chini ya mpango Wake, kile ambacho tumebakisha baada ya kutoa zaka kitaenda mbali zaidi kuliko vyote bila baraka Zake. Kweli, hatuwezi kumudu kutotoa zaka!

**Maswali ya Maswali**

**1. Neno "zaka" kwa kweli linamaanisha "kumi." (1)**

_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**2. Zaka tayari ni ya Mungu. (1)**

_____ Kweli.
_____ Uongo.

**3. Mimi Sitoi zaka kama sirudishi sehemu ya kumi ya mapato yangu kwa Mungu. (1)**

_____ Kweli.
_____ Uongo.

**4. Yesu aliidhinisha kurudisha zaka. (1)**

_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**5. Ni ipi kati ya zifuatazo ni miongozo na kanuni za Biblia za kutoa kwa hiari? (5)**

_____ Toa ikiwa una chochote kilichosalia.
_____ Toa kwa furaha.
_____ Toa kwa wingi.
_____ Toa ili ujisikie vizuri.
_____ Toa jinsi Mungu alivyokufanikisha.

_____ Kutoa ni bora kuliko kupokea.
______Mungu atarudisha zaidi ya unavyotoa.
_____ Toa kama unapenda.
_____ Toa ili watu wasifikiri kuwa wewe ni bahili.

**6. Kulingana na Biblia, chanzo cha mapato kwa watumishi wa injili kinapaswa kuwa (1)**
_____ Michezo ya Bingo.
_____ Mauzo ya tembo weupe.
_____ Zaka.
_____ Mauzo ya chapati.
_____ Bahati nasibu au michezo fulani.

**7. Ni mababu gani wa Agano la Kale ambao walirudisha zaka kabla ya siku za Musa waliotajwa katika Mwongozo huu wa Somo? (2)**
_____ Adamu.
_____ Yakobo.
_____ Nuhu.
_____ Isaka.
_____ Ibrahimu.
_____ Methusela.

**8. Kulingana na Malaki 3:8, watu wasiotoa zaka na sadaka wana hatia ya dhambi gani? (1)**
_____ Ibada ya sanamu.
_____ Kuivunja Sabato.
_____ Kuua.
_____ Ujambazi.

**9. Kulingana na kitabu cha Waebrania, ni nani hasa anapokea pesa zetu tunapotoa zaka? (1)**
_____ Mchungaji.
_____ Wahitaji.
_____ Yesu, Kuhani wetu Mkuu wa mbinguni.

**10. Kulingana na 2 Timotheo 3:1-7, moja ya dhambi 20 za siku za mwisho ambazo zitawafungia watu nje ya ufalme wa Mungu ni kutamani. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**11. Kuleta zaka katika ghala la Mungu kunamaanisha (1)**
_____ Kuitumia kununua vitabu vya kiroho.
_____ Kuitumia kwa sababu yoyote ya kiroho au kusaidia yatima na wajane au ndugu.
_____ Kuitoa kwa hazina ya kanisa la Mungu.

**12. Mungu anawaahidi nini waaminifu zaka katika Malaki 3:10? (1)**

_____ Hataugua kamwe.
_____ Hatapoteza kazi yake kamwe.
_____ Atapokea baraka nyingi kuliko anavyoweza kushughulikia.

**13. Mungu aliwapa Adamu na Hawa mtihani kuhusu kula kipande cha tunda. Kulingana na Mwongozo huu wa Somo, ni mtihani gani sawa na huo Anaowapa watu Wake leo? (1)**
_____ Kusoma Biblia kila siku.
_____ Kushuhudia.
_____ Kurudisha zaka.
_____ Kuomba.

**14. Zaka ilikuwa ni sehemu ya sheria ya Musa, ambayo iliishia pale msalabani. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**15. Je, Mungu hupimaje karama zangu Kwake? (2)**
_____ Kwa kiasi ninachotoa.
_____ Kwa kiasi cha dhabihu.
_____ Kwa moyo na mtazamo ninaokuwa nao nikitoa.

**16. Uwakili mwaminifu hauhusishi tu kutumia vizuri pesa zangu, bali pia muda ninaotumia katika shughuli kama vile maombi, kushuhudia, kufuata nyayo za Kristo, Kuwapa wengine habari njema, kujifunza Maandiko, na kuwasaidia wengine. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

## Upendo Unaobadilika

## Somo la 26

Kuwa katika upendo hubadilisha kila kitu. Kwa mfano, mwanamke kijana alikuwa akisoma kitabu kikubwa kwa ajili ya kozi yake ya fasihi ya Kiingereza ya chuo kikuu. Alipata jambo hilo lote kuwa la kuchosha sana na hakuweza kukazia fikira wakati akisoma. Lakini basi alikutana na profesa kijana kwenye chuo kikuu, na wakapendana haraka. Muda mfupi baadaye, aligundua mpendwa wake ndiye mwandishi wa kitabu ambacho alikuwa amehangaika nacho. Usiku huo alikesha na 'kubugia' kitabu kizima kwa mshangao, "Hiki ndicho kitabu bora zaidi ambacho nimewahi kusoma!" Ni nini kilibadili mtazamo wake? Upendo ulifanya hilo. Vivyo hivyo, wengi leo huona Maandiko kuwa ya kuchosha, yenye kukandamiza, na yasiyopendeza. Lakini hiyo yote hubadilika unapopendana na Mwandishi. Tazama jinsi gani katika Mwongozo huu wa Mafunzo utachangamsha moyo!

**<u>Yesu Ndiye mwandishi wa Maandiko.</u>**

**1. Mwandishi wa Maandiko ni nani?**
"Manabii wameuliza na kuchunguza kwa bidii, ... wakichunguza ni wakati gani, au ni wakati wa namna gani Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao alimaanisha, alipotangulia kuyashuhudia mateso ya Kristo, na utukufu utakaofuata. 1 Petro 1:10, 11 .

**Jibu:** Mungu wa Biblia (hata Agano la Kale) karibu mara zote ni Yesu Kristo. Yesu aliumba ulimwengu ( Yohana 1:1-3 , 14 Wakolosai 1:13-17 ), Aliandika zile Amri Kumi ( Nehemia 9:6 , 13 ),Alikuwa Mungu wa Waisraeli ( 1 Wakorintho 10:1-4 ), na Aliongoza Maandiko ya manabii au alivuvia ( 1 Petro 1:10 ) , 11 ).

Kwa hiyo, Yesu Kristo Ndiye Mwandishi wa Maandiko.
Yesu anawapenda watu wa dunia kwa upendo wa milele.

**2. Yesu ana mtazamo gani kuelekea watu wa dunia?**
"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16 .

**Jibu:** Yesu anatupenda sisi sote kwa upendo usioelezeka, usio na kikomo, unaopita ufahamu.
Yesu alikufa kwa ajili yetu sote, ingawa hakuna hata mmoja wetu aliyestahili.

**3. Kwa nini tunapaswa kumpenda Yesu?**
"Sisi tunampenda kwa sababu Yeye alitupenda sisi kwanza." 1 Yohana 4:19 . "Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu." Warumi 5:8 .

**Jibu:** Tunapaswa kumpenda kwa sababu alitupenda kiasi cha kufa kwa ajili yetu—tulipokuwa bado adui Zake.

**4. Ndoa yenye mafanikio na maisha ya Kikristo yanafanana katika mambo gani?**
"Na lolote tuombalo, twalipokea Kwake, kwa kuwa twazishika amri
Zake, na kuyatenda yapendezayo machoni Pake." 1 Yohana 3:22 .

**Jibu:** Katika ndoa nzuri kuna mambo fulani ya lazima, kama vile uaminifu kwa mwenzi wa ndoa. Mambo mengine yanaweza yasionekane kuwa makubwa, lakini yakimpendeza mwenzi ni muhimu. Ikiwa hayapendezi, yanapaswa kukomeshwa. Ndivyo ilivyo na maisha ya Kikristo. Amri za Yesu ni za lazima.
Lakini katika Maandiko Yesu pia ametueleza kanuni za mwenendo zinazompendeza. Kama ilivyo katika ndoa nzuri, Mkristo hupata shangwe au furaha tele kufanya mambo yanayomfurahisha Yesu, Yule anayempenda. Pia anaepuka mambo yasiyompendeza.
Kufanya mambo yanayompendeza Yesu humletea mtu furaha kubwa na maisha tele.

**5. Yesu anasema nini matokeo ya kufanya mambo yanayompendeza?**
"Mkizishika amri Zangu, mtakaa katika pendo Langu; ... Hayo nimewaambia, ili furaha Yangu ikae ndani yenu, na furaha yenu iwe kamili." Yohana 15:10 , 11 .

**Jibu:** Ibilisi anadai kwamba kufuata kanuni za Kikristo ni upuuzi, ujinga, kujidhalilisha, na kukazania sheria kwa kupitiliza etc. Lakini Yesu anasema inaleta utimilifu wa furaha ( Yohana 15:10 , 11 ) na uzima tele ( Yohana 10:10 ). Kuamini uongo wa shetani huleta maumivu ya moyo na kuwanyima watu maisha ambayo "yanaishi Kweli."
Kanuni za Biblia za Yesu kuhusu maisha ya Kikristo hutulinda kutokana na maeneo hatari ya Shetani.

**6. Kwa nini Yesu anatupa kanuni hususa za maisha ya Kikristo?**
**Jibu:** Kwa sababu wao:

A. Ni kwa faida yetu wenyewe siku zote ( Kumbukumbu la Torati 6:24 ). Kama vile wazazi wazuri wanavyowafundisha watoto wao kanuni nzuri, ndivyo Yesu anavyowafundisha watoto Wake kanuni nzuri.

B. Zinaweka kwa ajili yetu ulinzi dhidi ya dhambi ( Zaburi 119:11 ). Kanuni za Yesu hutulinda tusiingie katika maeneo hatari ya Shetani na dhambi.

C. Hutuonyesha jinsi ya kufuata nyayo za Kristo ( 1 Petro 2:21 ).

D. Hutuletea furaha ya kweli ( Yohana 13:17 ).

E. Hutupa nafasi ya kuonyesha upendo wetu Kwake ( Yohana 15:10 ).

F. Tusaidie kuwa kielelezo sahihi kwa wengine ( 1 Wakorintho 10:31-33 ; Mathayo 5:16 ).

Ninapopenda mambo ya ulimwengu, ninakuwa adui wa Mungu.

7. **Kulingana na Yesu, Wakristo wanapaswa kujihusishaje na uovu wa ulimwengu na ulimwengu?**

**Jibu:** Amri na ushauri Wake ni wazi na mahususi:

A. Usiipende dunia wala mambo ya dunia. Mambo ya dunia ambayo si ya Mungu ni: (1) tamaa ya mwili, (2) tamaa ya macho, na (3) kiburi cha uzima ( 1 Yohana 2:16 ) . Dhambi zote zinaangukia katika moja au zaidi ya makundi haya matatu. Shetani anatumia njia hizi tatu ili kutuvuta tuipende dunia. Ninapoanza kuupenda ulimwengu, ninakuwa adui wa Mungu ( 1 Yohana 2:15 , 16 . Yakobo 4:4 ).

B. Ni lazima nijiweke bila doa kutoka kwa ulimwengu ( Yakobo 1:27 ).
Mkristo anapaswa kupinga kwa uthabiti mambo ya ulimwengu, au atapotoshwa na Shetani.

**8. Mungu anatupa onyo gani la uharaka kuhusu ulimwengu?**

**Jibu:** Yesu anawaonya Wakristo, "Msiifuatishe namna ya dunia hii." Warumi 12:2 . Tafsiri ya Phillips yasema hivi: "Usiruhusu ulimwengu unaokuzunguka ukufinyange katika umbo lake lenyewe."* Ibilisi haegemei upande wowote. Anamsukuma kila Mkristo kila mara. Kupitia Yesu ( Wafilipi 4:13 ), ni lazima nipinge kwa uthabiti mapendekezo ya shetani, naye atanikimbia ( Yakobo 4:7 ). Dakika ninaporuhusu "kunibana" kwa sababu nyingine yoyote kwa kushawishi mwenendo wangu, ninaanza kuingia katika uasi bila kuonekana. Tabia za Kikristo hazipaswi kuamuliwa kwa hisia na mwenendo wa wengi, yaani wengi wape, kwani Mungu hatumii maoni ya watu wengi au demokrasia, maana inawez akuwa na makosa, bali anatumia serikali Yake ya upendo, na Maandiko Yake kuwa kigezo,

Lazima tulinde kwa uangalifu mawazo yetu, kwa sababu mawazo huwa maneno, kisha huwa vitendo.

**9. Kwa nini tunahitaji kulinda mawazo yetu?**
"maana Aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo." Mithali 23:7 .

**Jibu:** Ni lazima tuchunge mawazo yetu, kwa sababu mawazo yanaumba maneno, na tabia. Mungu anataka kutusaidia "kuteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo." 2 Wakorintho 10:5 . Lakini Shetani anataka sana kuleta "ulimwengu" katika mawazo yetu. Anaweza kufanya hivi kupitia hisia zetu tano tu—hasa kuona na kusikia. Yeye hukazia macho yake na sauti juu kwetu sote na, tusipokataa mara kwa mara anachotaka tutazame au kusikiliza,yeye atatuelekeza kwenye njia pana iongozayo kwenye uharibifu. Biblia iko wazi. Tunakuwa kama vile vitu tunavyoviona na kuvisikia mara kwa mara ( 2 Wakorintho 3:18 ).
Ni lazima Wakristo waepuke muziki wowote unaopunguza tamaa ya kuishi maisha ya mbingu.

**10. Zipi ni baadhi ya kanuni za maisha ya Kikristo? Au tuna kichujio gani kinachochuja kile tunachopaswa kufanya na kuacha? Fungu hili ndilo kichujio.**
"Mambo yoyote yaliyo ya Kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema, ukiwapo wema wowote, ikiwako sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo. " Wafilipi 4:8 .

**Jibu:** Wakristo lazima wajitenge na mambo yote ambayo si ya Kweli, si ya uaminifu, si ya haki, si safi, si ya kupendeza, na si yenye sifa njema. Waepuke yaani uwe moto wa kuotea mbali:

A. Ukosefu wa uaminifu wa kila aina - kudanganya, kusema uwongo, kuiba, kutotenda haki, nia ya kudanganya, kashfa, na usaliti.

B. Uchafu wa kila aina. Hii inahusisha uasherati, uzinzi, ngono na watu wa ukoo wako wa kribu, ugoni, ndoa za jinsia-moja, upotovu wa kila aina, kupiga punyeto au masturbation, ponografia, lugha chafu, mazungumzo machafu, futuhi za matusi

au kejeli zenye lugha mbaya, dansi za kijamii kama madisko, matusi, nyimbo au muziki mbovu, na mambo mengi yanayoonyeshwa kwenye televisheni na katika majumba ya sinema.

C. Mahali ambapo hatutawahi kumwalika Yesu atusindikize, kama vile vilabu vya usiku, mikahawa, kasino za kamari, viwanja vya mbio, n.k.

Hebu tuchukue dakika chache kufafanua hatari za muziki maarufu, dansi, televisheni, video na ukumbi wa michezo.

**Muziki na Wimbo**

Aina nyingi za muziki wa kilimwengu (rapu, country music, pop, roki, muziki wa diamond, mdundo mzito, muziki wa kisasa na wa dansi) zimenaswa kwa kiasi kikubwa na Shetani. Maneno hayo mara nyingi hutukuza uovu na kuharibu matamanio ya mambo ya kiroho na yanahusisha mambo ya ngono kwa uvaaji na kucheza kwa kukosa adabu kama vile sindimba, ngoma za kutingisha mwili, na wanaume na wanawake wasio katika mahusiano ya ndoa kukumbatiana na kucheza pamoja, Watafiti wamegundua mambo fulani yenye kupendeza kuhusu nguvu za muziki:

(1) Huingia kwenye ubongo kupitia hisia, na hivyo inatoka nje ya uwezo wa kufikiri bypasses the frontal lobe.

(2) Inaathiri kila kazi ya mwili.

(3) Inaweza kubadilisha mapigo ya moyo, kasi ya kupumua, na miitikio bila mtu kutambua.

(4) Midundo ya dansi ya Syncopated hubadilisha hali na kuunda hali ya kustaajabisha kwa msikilizaji.

Hata bila maneno, muziki wenyewe una uwezo wa kushusha hisia, tamaa, na mawazo ya mtu. Wanamuziki wa kilimwengu wa roki hukubali hili waziwazi. Kiongozi wa Rolling Stones Mick Jagger alisema: "Unaweza kuhisi adrenalini ikipitia kwenye mwili wako. Ni aina ya ngono." 1 John Oates wa Hall and Oates alisema kuwa "Rock 'n' Roll ni ngono 99%. "2 Je, muziki kama huo utampendeza Yesu? Wapagani waongofu kutoka ng'ambo wanatuambia kwamba muziki wetu wa kisasa wa bendi za kilimwengu ni aina ile ile waliyotumia katika uchawi na ibada ya shetani!

Jiulize: "Ikiwa Yesu angekuja kunitembelea, ni muziki gani ningejisikia vizuri kumwomba asikilize pamoja nami?" Muziki wowote ambao huna uhakika nao unapaswa kuachwa. (Kwa uchambuzi wa kina wa muziki ulioharibika, wa kilimwengu, tunapendekeza Vidokezo kuhusu Muziki vya Carol na Louis Torres, ambavyo vinaweza kununuliwa kutoka huduma ya Amazing facts.) Tunapompenda Yesu, Yeye hubadilisha tamaa zetu za muziki. "Amenitia wimbo mpya kinywani mwangu, za sifa kwa Mungu wetu; wengi wataona na kuogopa, na watamtumaini Bwana." Zaburi 40:3 . Mungu amewaandalia watu Wake muziki mwingi mzuri unaotia moyo, kuburudisha, kuinua, na kuimarisha uzoefu wa Kikristo. Wale wanaokubali muziki wa shetani

unaodhalilisha kama kibadala wanakosa mojawapo ya baraka bora zaidi maishani. Muziki ulianzishwa kwaajili ya ibada, kwa kumtukuza Mungu, ila sasa umetoka mbali.

**Kucheza**

Dansi bila shaka inampeleka mbali na Yesu na kiroho. Waisraeli walipocheza kuzunguka ndama wa dhahabu, walimsahau Mungu ( Kutoka 32:17-25 ). Binti ya Herodia mwovu alipocheza mbele ya Mfalme Herode, Yohana Mbatizaji alikatwa kichwa ( Mathayo 14:2-12 ). Ona takwimu hizi zenye kushtua: Kasisi Mkatoliki katika New York alisema kwamba robo tatu ya wasichana ambao wamekiri uzinzi kwake waliweka lawama juu ya kucheza dansi ambako kuliwaponza. Mapadre wengine wamesema kwamba robo tatu ni chini sana wanakadiria tisa ya kumi ya muziki kuhusika na ngono potofu au uhalifu. Kumbuka, ikiwa Kristo anaweza kushiriki katika shughuli na wewe, uko salama. Ikiwa sivyo, kaa mbali nayo.

**TV, Video, na Ukumbi wa Kuigiza**

Je, mambo unayotazama kwenye televisheni na video au katika jumba la maonyesho yanavuta hali yako kwenda kwenye mambo ya giza chini au ya juu zaidi? Je, yanakuongoza katika upendo mkuu kwa Yesu, au kwa ulimwengu? Je, unamtukuza Yesu, au maovu ya shetani? Katika siku zetu hata watu wasio na dini na wasio Wakristo wanazungumza dhidi utayarishaji wa TV na filamu nyingi. Shetani ameteka macho na masikio ya mabilioni ya watu na, kwa sababu hiyo, anageuza ulimwengu upesi kuwa dimbwi la ukosefu wa maadili, uhalifu, ugaidi, na kukosa tumaini. Uchunguzi mmoja ulisema kwamba bila TV "mauaji 10,000 yangepungua kila mwaka Marekani, ubakaji 70,000 ungepungua, na mashambulio ya majambazi yangekuwa 700,000 pungufu." 3 Yesu, ambaye anakupenda, anakuomba uondoe macho yako mbali na vidhibiti-fikira vya Shetani na uyaweke juu Yake. Anasema, "Niangalieni Mimi, nanyi mpate kuokolewa." Isaya 45:22 .

1 Newsweek, "Mick Jagger na Mustakabali wa Mwamba", Januari 4, 1971, p. 47.

2Circus magazine, Januari 31, 1976, p. 39.

3Newsweek, "Vurugu, Reel to Reel", Desemba 11, 1995, p. 47.
Mwongozo salama wa kutazama TV ni kuuliza, "Je, ningejisikia vizuri kumwalika Yesu kutazama kipindi pamoja nami?"

**11. Yesu anatupa orodha gani iliyo wazi ambayo tunaweza kutumia ili kutazama televisheni?**

"Basi matendo ya mwili ni dhahiri kabisa: uasherati, uchafu na uchafu, ibada ya sanamu na uchawi, hasira ya ugomvi, husuda, hasira, ubinafsi, mafarakano, fitina, wivu, ulevi, karamu. , na kadhalika. Nawaonya, kama nilivyowaonya hapo awali, kwamba watu wafanyao hivyo hawataurithi ufalme wa Mungu. Wagalatia 5:19-21,

**Jibu:** Maandiko yako wazi sana ka mtu kutoelewa. Ikiwa familia itapiga marufuku programu zote za TV zinazoonyesha au kuunga mkono dhambi zozote zilizo hapo juu, kutakuwa na uchache sana wa kutazama mtandao. Ikiwa Yesu angekuja kukutembelea, ni vipindi gani vya televisheni ungejisikia huru kumwomba

atazame nawe? Maonyesho mengine yote labda hayafai kutazamwa na Kikristo.

Chaguo langu la programu za TV na, kwa kweli, mwenendo wangu wote lazima uongozwe na maneno ya Maandiko, na sio hisia zangu mwenyewe.

**12. Katika siku hii ya kujiamulia, kufikiri kwa kujitegemea, wengi wanahisi kuwa na uwezo kabisa wa kufanya maamuzi ya kiroho bila maoni kutoka kwa mtu yeyote, au katika ndani Yesu. Yesu anasema nini kuhusu watu kama hao?**

**Jibu:** Sikiliza kauli za Yesu zisizo na shaka: "Msifanye sawasawa na mambo yote tuyafanyayo hapa leo, kila mtu anavyoona ni sawa machoni pake mwenyewe." Kumbukumbu la Torati 12:8 . "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti." Mithali 16:25 . "Njia ya mpumbavu ni sawa machoni pake mwenyewe; bali yeye asikilizaye shauri ana hekima." Mithali 12:15 . "Anayetumainia moyo wake [akili] ni mpumbavu." Mithali 28:26 .

**13. Yesu anatupa maonyo gani mazito kuhusu kielelezo na uvutano wa maisha yetu?**

"Lakini yeyote atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, ingekuwa afadhali afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari." Mathayo 18:6 . Hebu "mtu yeyote asiweke kikwazo au sababu ya kuanguka katika njia ya ndugu yake." Warumi 14:13 . "Hakuna hata mmoja wetu anayeishi kwa nafsi yake." Warumi 14:7 .

**Jibu:** Sote tunatarajia viongozi, watu wenye ushawishi, wanariadha mashuhuri, na watu wengine wanaojulikana sana wawe mfano mzuri na kutumia ushawishi wao kwa busara--kulipa kile kinachoitwa "deni kwa jamii". Lakini katika ulimwengu wa leo, mara nyingi tunakatishwa tamaa na matendo yenye kuchukiza na ya kutowajibika ya watu mashuhuri. Yesu anasema waziwazi katika Warumi 1:14 kwamba Wakristo, wanaomwakilisha Yeye na ufalme Wake, hakika wana deni fulani kwa wengine. Na anatahadharisha kwa uthabiti kwamba Wakristo wanaopuuza mvuto wao na mfano wao, na hivyo kuwapoteza watu, hawataingia katika ufalme Wake.

Mungu anawauliza watu Wake kuweka kando mapambo na vito. Kuwapikia wengine pombe, au kutangaza kuhusu sigara, nao ni uovu ambao Mungu hakubalini nao, kwani mtu anamuumiza jirani yake.

**14. Yesu ana kanuni gani za mwenendo kuhusu mavazi na vito?**

**Jibu:** A. Vaa kwa kiasi. Ona 1 Timotheo 2:9 . Kumbuka kwamba ulimwengu unaletwa maishani mwetu kwa tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, hivyo kaa chonjo, ( 1 Yohana 2:16 ). Mavazi yasiyo ya kiasi yahusisha yote matatu na ni marufuku kwa Mkristo kuyavaa. Tuandikie tukutumie kitabu cha mavazi ya staha bure.

B. Weka mapambo na vito pembeni. "Kiburi cha maisha" ndio shida kubwa hapa. Wafuasi wa Yesu wanapaswa kuonekana tofauti. Kuonekana kwao kunashuhudia na kutuma nuru kwa wengine ( Mathayo 5:16 ). Kujifanya huvutia umakini na kujiinua.

Katika Biblia, ni ishara ya kurudi nyuma na uasi. Yakobo na familia yake walipoweka wakfu tena maisha yao kwa Bwana, walizika vito vyao duniani ( Mwanzo 35:1 , 2 , 4 ). Waisraeli walipokuwa karibu kuingia katika nchi ya ahadi, Bwana aliwaamuru wavue mapambo yao ( Kutoka 33:5 , 6 ). Katika Isaya sura ya 3, Mungu anasema waziwazi kwamba katika kuvaa vito (bangili, pete, pete, n.k. kama ilivyoorodheshwa katika mistari 19-23), watu Wake walikuwa wakitenda dhambi (mstari wa 9).

Katika Hosea 2:13 , Bwana anasema kwamba Israeli walipomwacha, walianza kuweka heleni na bangili au mikufu. Katika 1 Timotheo 2:9 na 1 Petro 3:3 , Paulo na Petro wote wanatufahamisha kwamba watu wa Mungu hawatajipamba kwa dhahabu, lulu, na mavazi ya gharama. Tafadhali ona kwamba Petro na Paulo walizungumza kuhusu mapambo ambayo Mungu anataka watu Wake wavae: "Roho ya upole na utulivu" ( 1 Petro 3:4 ) na "matendo mema" ( 1 Timotheo 2:10 ). Yesu anahitimisha kwa kuashiria kanisa Lake la kweli katika Ufunuo 12:1 kama mwanamke safi aliyevikwa jua (mng'ao na haki ya Yesu) na kanisa lililoasi kama kahaba aliyevikwa dhahabu, mawe ya thamani na lulu (Ufunuo 17:3) . , 4). Mungu anawauliza watu Wake wajitenge na Babeli ( Ufunuo 18:2-4 ) na yote inachosimamia - ikiwa ni pamoja na vito vinavyovutia watu binafsi - na badala yake kujivika haki ya Yesu. Tunapompenda Yesu, ni furaha na raha kuu kuishi mtindo Wake wa maisha.
Kitu chochote kinachopunguza upendo wangu kwa mambo ya kiroho kinakuwa sanamu.

**15. Mwenendo na utii vinahusianaje na wokovu?**
**Jibu:** Utii na mwenendo wa Kikristo ni uthibitisho, au ushahidi, kwamba nimeokolewa na Yesu Kristo ( Yakobo 2:20-26 ). Ukweli wa mambo ni kwamba isipokuwa mtindo wa maisha wa mtu ubadilike baada ya uongofu, uwezekano mkubwa uongofu huo haukuwa wa kweli. Mtu aliyeongoka atapata furaha yake kuu katika kugundua mapenzi ya Yesu katika kila jambo na kwa kufuata kwa furaha pale Bwana anapoongoza.

**Jihadhari na Ibada ya Sanamu**
Waraka wa kwanza wa Yohana unazungumza kuhusu mwenendo wa Kikristo. Mwishoni mwake ( 1 Yohana 5:21 ), Yesu anatuonya kupitia mtumishi Wake Yohana tujiepushe na sanamu. Mwalimu anarejelea kitu chochote kinachoingilia au kupunguza upendo wangu Kwake, kama vile muziki, mitindo, uasherati, ngono potofu, mali, mapambo, aina mbaya za burudani, n.k. Tunda la asili, au matokeo, ya uongofu wa kweli ni kumfuata Yesu kwa furaha na fuata mtindo Wake wa maisha. Watu ambao hawajajitoa kikamilifu kwa Yesu hawataelewa kamwe mtindo wa maisha wa Mkristo, na hatupaswi kuwatarajia kuelewa.

**16. Je, twapaswa kutazamia kila mtu atazame kwa upendeleo mtindo wa maisha wa Kikristo?**

**Jibu:** Hapana. Yesu alisema kwamba mambo ya Mungu ni upuzi kwa mwanadamu wa asili kwa sababu hayatambuliwi kiroho ( 1 Wakorintho 2:14 ). Yesu anaporejelea mwenendo, anaweka kanuni kwa wale wanaotafuta kuongozwa na Roho Wake. Watu Wake watakuwa na shukrani na watafuata ushauri Wake kwa furaha.

Wengine wanaweza wasielewe au kuidhinisha. Ila wale wasiojua ambao wako mamilioni, Mungu atakapowajulisha, wataacha uovu huu. Nguo tunazivaa kwa vile lilikuwa agizo la Mungu, kwamba alikuwa anatuvika kwa utukufu Wake na baada ya dhambi tupo uchi, inabidi tuvae nguo, na si vipande vidogo vidogo tu. Haruni aliambiwa kwamba mapaja yake ni utupu, ayafunike, asije akakatiliwa mbali Mtu anayekataa mtindo wa maisha wa Yesu atakuwa na huzuni mbinguni. Hapatamfaa pale, atakuwa anataka kubishana na kuleta uasi, hata akiruhusiwa aende huko, ataanza vita tena na dhambi haitainua kichwa humo, Nahum 1:9

**17. Mtu anayekataa viwango vya Yesu vya mwenendo wa Kikristo angeionaje mbingu kama angeenda huko?**

**Jibu:** Mtu kama huyo atakuwa mnyonge mbinguni. Angelalamika kwamba hakukuwa na vilabu vya usiku, vileo, ponografia, makahaba, muziki wa uasherati, vitabu vichafu, lugha chafu, na kucheza kamari. Mbingu ingekuwa "Jehanamu" kwa wale ambao hawajaunda uhusiano wa kweli wa upendo na Yesu. Hii ndiyo sababu viwango vya Kikristo havina maana kwao ( 2 Wakorintho 6:14-17 ).

**18. Ninawezaje kufuata na kufuata miongozo hii ya Biblia bila kuonekana kama mfarisayo, mwenye kuhukumu, au mwenye kufuata sheria kwa kupitiliza -legalist or liberal?**

**Jibu:** Kila kitu tunachofanya kinapaswa kuwa na wazo moja akilini: kuonyesha upendo na heshima kwa Yesu ( 1 Yohana 3:22 ). Yesu atakapoinuliwa na kuonyeshwa kwa watu ( Yohana 12:32 ), watu watavutwa Kwake. Swali letu moja linapaswa kuwa, "Je, huyu atamheshimu Yesu? na mimi?"

Yesu Yuko pamoja nawe na mimi ( Mathayo 28:20 ), na anaona kila kitu tunachofanya. Lazima nihisi uwepo wa Yesu katika kila nyanja na shughuli za maisha. Ninapokaa Naye kwa uangalifu, ninakuwa kama Yeye ( 2 Wakorintho 3:18 ). Kisha watu watakapokuwa pamoja  Naye, wataitikia kama walivyowajibu wanafunzi wa kale: "Wakastaajabu na wakawatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu. Matendo 4:13 . Wakristo wanaoishi hivyo hawatawahi kuwa mafarisayo, watu wanaoishika sheria kwa kupitiliza na kuwahukumu wengine kama mfarisayo.

Katika siku za Agano la Kale, watu wa Mungu walikuwa wanajiingiza katika ukengeufu wa kila mara kwa sababu walichagua kuishi kama majirani zao wapagani badala ya kufuata mtindo wa kipekee wa maisha ambao Mungu aliwawekea ( Kumbukumbu la Torati 31:16 ) Waamuzi 2:17 1 Mambo ya Nyakati 5:25 Ezekieli 23:30 ). Hili ni kweli hata leo. Hakuna awezaye kutumikia mabwana wawili ( Mathayo 6:24 ). Wale wanaoshikamana na ulimwengu na mtindo wake wa maisha watafinyangwa polepole na Shetani wakubali hisia na tamaa zake, na hivyo kuingia mkakati wa kupotea. Wale wanaofuata kanuni za Yesu za mwenendo wa Kikristo watabadilishwa kuwa sura Yake na kutayarishwa kwa ajili ya mbinguni. Hakuna kusimama katikati.

**19. Ninataka kumpenda Kristo sana hivi kwamba kufuata kanuni Zake kwa maisha ya Kikristo itakuwa furaha na furaha.**

**Jibu:**

**Maswali ya Kucheua**

**1. Ninajua kile ambacho Mungu angependa nifanye, lakini sijisikii kuwa niko tayari kuanza kukifanya. Unashauri nini?**

Anza kuifanya mara moja! Kamwe usitegemee hisia. Mungu huongoza kupitia Maneno ya Maandiko ( Isaya 8:20 ). Hisia mara nyingi husababisha upotovu. Viongozi wa Kiyahudi waliona kuwa wanapaswa kumsulubisha Yesu, lakini walikosea. Wengi watahisi kuokolewa katika ujio wa pili wa Yesu, lakini wao, badala yake, watapotea ( Mathayo 7:21-23 ). Ibilisi huathiri hisia. Nikitegemea hisia zangu, ataniongoza kwenye uharibifu.

**2. Nina shida. Nataka sana kufanya jambo fulani. Ninatambua, hata hivyo, kwamba kwa sababu ya kuonekana kwake, wengine wanaweza kuhisi ninafanya uovu. Nifanye nini?**

Biblia iko wazi. Inasema, “Jiepusheni na uovu wote.” 1 Wathesalonike 5:22 . Na mtume Paulo alisema kwamba ikiwa ulaji wake wa vyakula vya nyama utamchukiza mtu, kamwe yeye kugusa vyakula hivyo tena ( 1 Wakorintho 8:13 ). Pia alisema kwamba ikiwa angepuuza hisia za mtu aliyeudhiwa na kuendelea kula vyakula vya nyama, atakuwa anatenda dhambi.

**3. Inaonekana kwangu kwamba makanisa yanaorodhesha mambo mengi sana ambayo lazima nifanye na mambo mengi sana ambayo ni lazima nisiyafanye. Hili linanitia wazimu. Je, kumfuata Yesu si jambo la maana sana?**
Ndiyo, kumfuata Yesu ndilo jambo la maana. Hata hivyo, kumfuata Yesu kunamaanisha kitu kimoja kwa mtu mmoja na kitu tofauti kabisa na mwingine. Njia pekee iliyo salama ya kujua maana ya kumfuata Yesu ni kugundua kile Yesu anachosema katika Biblia kuhusu swali lolote kuhusu kutenda mema. Wale wanaofuata amri za Yesu kwa upendo siku moja wataingia ufalme Wake hivi karibuni ( Ufunuo 22:14 ). Wale wanaofuata sheria zilizotungwa na wanadamu watapotea na wanaweza kuongozwa mbali na ufalme Wake ( Mathayo 15:3-9 ).

**4. Matakwa fulani machache ya Mungu yanaonekana kuwa yasiyo na maana na yasiyo ya lazima kwangu. Sielewi kwa nini ni muhimu. Unashauri nini?**
Watoto mara nyingi huhisi kuwa baadhi ya matakwa ya wazazi wao (km “Usicheze barabarani”) hayana utashi au ni ya kijinga. Lakini katika miaka ya baadaye, mtoto atawashukuru wazazi kwa mahitaji hayo. Sisi ni “watoto” katika kushughulika na Mungu, kwa sababu mawazo na matendo Yake yako juu sana kuliko yetu kama vile mbingu zilivyo juu ya dunia ( Isaya 55:8 , 9 ). Tunahitaji kumwamini Baba yetu wa mbinguni Mwenye upendo katika maeneo machache ambayo huenda hatuelewi na kuacha “kucheza barabarani” ikiwa Yeye anataka hivyo. Yeye hatatunyima kitu

chochote kizuri ( Zaburi 84:11 ). Ninapokuwa katika upendo wa kweli na Yesu, nitampa faida kutenda hata lile nililo na shaka nalo ambalo amelisema na kufanya mapenzi Yake hata kama sielewi kwa nini kila wakati. Kuzaliwa upya ni ufunguo katika kutii kila kitu. Biblia inasema nitakapozaliwa mara ya pili kweli, kuushinda ulimwengu halitakuwa tatizo kwa sababu mtu aliyeongoka atakuwa na imani na matumaini ya kumfuata Yesu kwa furaha katika kila jambo ( 1 Yohana 5:4 ) . Umimi au kujijali kutakwisha na atasikia Sauti ya Yesu kwanza. Kukataa kumfuata kwa sababu sielewi sababu Zake kunaonyesha ukosefu wa kumwamini Mwokozi wangu.

**5. Je, nitafaidika kutokana na kanuni, sheria, na amri za Yesu zenye upendo?**

Kabisa! Hakika! Kila kanuni, kanuni, sheria, au amri ya Yesu hutoa baraka za pekee sana. Ushindi mkubwa zaidi wa bahati nasibu katika historia unakuwa duni ukilinganishwa na baraka nyingi za Mungu kwa watoto Wake watiifu. Hapa kuna faida chache tu zinazotokana na kufuata sheria za Yesu:

1. Yesu aanakuwa rafiki mwandami wa kibinafsi.

2. Yesu anakuwa mshirika katika biashara.

3. Uhuru kutoka kwa hatia.

4. Amani ya akili.

5. Uhuru kutoka kwa hofu.

6. Furaha isiyoelezeka.

7. Maisha marefu.

8. Uhakikisho wa makao mbinguni.

9. Afya bora.

10. Hakuna hangover ya kunywa pombe vichwa vikuume na kumaliza pesa na kuleta taabu.

Ongea juu ya utajiri wa mkristo na upige vigelegele! Mkristo wa kweli hupokea faida kutoka kwa Baba yake wa mbinguni, ambazo hata watu matajiri zaidi duniani hawawezi kuzinunua kamwe.

**6. Kuhusiana na viwango na mtindo wa maisha, je, nina wajibu wa kuwafundisha watu wengine kuhusu hayo?**

Kanuni bora zaidi kwa sisi kufuata ni kuhangaikia mtindo wetu wa maisha. “Jichunguzeni wenyewe,” Biblia inasema katika 2 Wakorintho 13:5 . Wakati mtindo wetu wa maisha ni kama inavyopaswa kuwa, mfano wetu hutumika kama shahidi

wa kimya na hatuhitaji kumhutubia mtu yeyote. Watu watatutazama na kujua hakika tunampenda Mungu. Bila shaka, wazazi wana daraka la pekee la kuwasaidia watoto wao waelewe jinsi ya kumfuata Yesu.

**7. Ni hatari gani kuu zaidi kwa Wakristo leo?**
Miongoni mwa hatari kubwa zaidi ni uaminifu uliogawanyika. Wakristo wengi wana mapenzi mawili yanayogawanya moyo: kumpenda Yesu, na kupenda ulimwengu na mazoea yake ya dhambi na anasa. Wengi sana, inaonekana, wanatamani kuona jinsi wanavyoweza kuufuata ulimwengu kwa ukaribu na bado wahesabiwe kuwa Wakristo. Hiyo Haitafanya kazi. Yesu alionya waziwazi kwamba hakuna mtu "awezaye kutumikia mabwana wawili." Mathayo 6:24 .

**8. Lakini je, si kuwa mfarisayo kwa kufuata sheria za Kikristo kwa kuptiliza 'legalist'?**
Isipokuwa mtu anafanya hivyo ili kuokolewa ndiyo mbaya, ila tunapaswa kufanya kwa vile tunampenda Mungu na jirani na hatutaki tulete fujo na huzuni kwa Mungu au kwa watu wengine. Wokovu huja tu kama zawadi ya kimuujiza, ya bure kutoka kwa Yesu. Wokovu kwa matendo (au mwenendo) sio wokovu hata kidogo. Hata hivyo, kufuata viwango vya Yesu vya mwenendo kwa sababu nimeokoka na kumpenda Yeye kamwe si ufarisayo.

**9. Je, viwango vya Kikristo vinahusika na amri ya Yesu ya kuacha nuru yetu iangaze?**
Hakika! Yesu anasema Mkristo wa kweli ni nuru ( Mathayo 5:14 ). Pia alisema, "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni." Mathayo 5:16 . Huisikii nuru; unaiona. Watu wataona nuru ya Mkristo ikiangazia kwa mwenendo wake, mavazi, chakula, mazungumzo, mtazamo, huruma, usafi, fadhili, na uaminifu (viwango vya Yesu). Wataulizia kuhusu mtindo wake wa maisha na, hivyo, mara nyingi wataongozwa kwa Kristo.

**10. Je, viwango vya Kikristo si vya tamaduni fulani? Je, havipaswi kubadilika na wakati?**
Desturi zinaweza kubadilika, lakini viwango vya Biblia hudumu. "Neno la Mungu wetu litasimama milele." Isaya 40:8 . Kanisa lazima liongoze, sio kufuata mitindo ya watu wa dunia. Halipaswi kuratibiwa na tamaduni, ubinadamu, au mwelekeo wa siku. Hatupaswi kulishusha kanisa kwenye viwango vya kibinadamu vinavyokosea, lakini badala yake, kufikia viwango vya Yesu. Wakati kanisa linapoishi, kunena, kuonekana, na kutenda kama ulimwengu, ni nani angeweza kuliendea ili kupata msaada? Yesu anatuma wito wa ufafanuzi kwa watu Wake na kanisa Lake, akisema, "Tokeni kati yao, na jitengeni ... wala msiguse kitu kilicho kichafu, nami nitawakaribisha." 2 Wakorintho 6:17 . Kanisa la Yesu halipaswi kuiga ulimwengu, bali kuukataa. "Dunia" imeharibu mabilioni. Kanisa lazima lisijiunge na ghasia zake. Kanisa lazima lisimame na kwa sauti ya neema lakini thabiti liwaite watu kumsikiliza Yesu na kufikia viwango Vyake. Wakati msikilizaji anapompenda Yesu na kumwomba adhibiti maisha yake, Mwokozi atafanya miujiza inayohitajika ili kumbadilisha na kumsindikiza kwa usalama hadi ufalme wa milele wa Mungu.

Hakuna njia nyingine ya kwenda mbinguni.Masihi ni Njia, Kweli na Uzima, leo ukisikia sauti Yake, mfuate, usijiulize ulize

**11. Hakika si kila dansi ni mbaya. Je! Daudi hakucheza mbele za Bwana?** Ni Kweli, sio dansi zote ni mbaya. Daudi aliruka na kucheza mbele za Bwana kama ishara ya sifa kwa baraka Zake nje ya hekalu( 2 Samweli 6:14-16 ). Pia, alikuwa akicheza peke yake si na mwanamke fulani waliyekumbatiana. Ngoma ya Daudi ilifanana na ile ya kilema aliyeruka kwa furaha baada ya kuponywa na Yesu ( Matendo 3:8-10 ). Kucheza, au kurukaruka vile, kunapendekezwa na Yesu kwa wale wanaoteswa ( Luka 6:22 , 23 ). Kucheza dansi pamoja na watu wa jinsia tofauti (kunaongoza kwenye ukosefu wa maadili na nyumba zilizovunjika) na dansi chafu (kama vile wavua nguo yaani strippers) ndizo aina zinazoshutumiwa na Biblia.

**12. Biblia inasema nini kuhusu watu kulaaniana na kuhukumiana?** "Msihukumu msije mkahukumiwa. Mathayo 7:1 , 2 . "Kwa hiyo huna la kujitetea, ewe mwanadamu, uwe yeyote umhukumuye mwingine; Warumi 2:1 . Hii inawezaje kuwa wazi zaidi?

Hakuna udhuru au uhalali wa kumhukumu mtu mwingine isipokuwa mimi mwenyewe. Yesu Ndiye Hakimu ( Yohana 5:22 ). Ninapowahukumu wengine, ninanyakua cheo cha Kristo kama hakimu na kuwa Mpinga Kristo mdogo ( 1 Yohana 2:18 )--wazo zito, kweli!

**Maswali ya Maswali**

**1. Kanuni za upendo za Yesu za mwenendo zina raha kuzifuata ninapompenda. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**2. Kufuata viwango vya Yesu vya mwenendo kwa sababu nimeokoka na kumpenda ni halali. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**3. Mwandishi halisi wa Biblia ni Yesu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**4. "Msiipende dunia" inamaanisha kwamba hatupaswi kupenda (1)**
_____ Nchi yetu.
_____ Dunia kama sayari yetu.
_____ Njia na mambo ya ulimwengu huu yenye dhambi, maovu, na yasiyo ya Mungu.

**5. Kwa nini Yesu anatupa amri, sheria, na sheria hususani? (5)**
_____ Kwa faida yetu siku zote.
_____ Tutajua jinsi ya kuweka mfano mzuri kwa wengine.

_____ Kutuibia uhuru wetu.
_____ Ili tuweze kufuata nyayo za Kristo.
_____ Ili kutulinda na dhambi.
_____ Ili kutuweka chini ya kidole gumba chake.
_____ Ili kutuletea furaha ya kweli.

**6. Kanuni mbili nzuri za kuamua mwenendo ufaao wa Kikristo ni kama ifuatavyo: (2)**
_____ Gundua kile ambacho Biblia inasema.
_____ Tazama ili kuona washiriki wa kanisa wanafanya nini.
_____ Shauriana na watu wa ramli.
_______ Nenda kwa hisia zako.
______Jiulize Yesu angefanya nini.

**7. Shetani anaweza kutufikia kupitia hisia zetu tano tu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**8. Yesu anatoa shauri na miongozo hususa kwa ajili ya sehemu gani za mwenendo wa Kikristo zilizoorodheshwa hapa chini? (5)**
_____ Jinsi tunavyovaa.
_____ Maisha yenye afya.
_____ Kupamba mwili.
_____ Mchezo wa Olimpiki wa kuteleza kwenye theluji.
_____ Kula na kunywa.
_____ Kuendesha ndege.
_____ Kununua nyumba.
_____ Mfano na ushawishi.

**9. Mwenendo na utii vinahusianaje na wokovu? (1)**
_____ Tunaokolewa kwa mwenendo na utii wetu.
_____ Mtu aliyeokoka anaweza kupuuza mwenendo na utii na bado akawa tayari kwa mbingu.
_____ Mwenendo na utii ni ushahidi kwamba mtu ameongoka, au amezaliwa mara ya pili.

**10. Nikikataa kuacha kitu ambacho Yesu ananiuliza niache—kama vile vito, mchumba mwovu, nguo zenye kuonyesha utupu, muziki wa roki, au kutazama vipindi viovu vya televisheni—Mungu huona kitu hicho kisichoachwa kuwa sanamu. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**11. Maisha ya Kikristo ni kama ndoa nzuri kwa kuwa mafanikio huja wakati lengo letu ni kumpendeza yule tumpendaye. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**12. Shetani huwaongoza watu katika dhambi ni njia zipi tatu kati ya zilizoorodheshwa hapa chini? (3)**

_____ Kuficha Biblia zao.
_____ Kiburi cha maisha.
_____ Kuandika jumbe angani.
_____ Tamaa ya mwili.
_____ Tamaa ya macho.

**13. Kulinda mawazo yetu ni muhimu, kwa sababu mawazo huwa matendo. (1)**

_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**14. Baadhi ya manufaa yaliyoahidiwa ya kumfuata Yesu kwa uaminifu ni kama ifuatavyo: (7)**

_____ Utajua jinsi ya kutabiri.
_____ Utaishi maisha marefu zaidi.
_____ Utakuwa furaha isiyoelezeka.
_____ Utakuwa na afya bora.
_____ Nywele zako hazitakuwa na mvi.
_____ Utakuwa milionea.
_____ Utahakikishiwa kuwa na makao mbinguni.
_____ Utakuwa na uhuru kutoka kwa woga.
_____ Utakuwa na Yesu kama rafiki wa kibinafsi.
_____ Utafurahia amani ya akili.

**15. Nifanye nini ikiwa mwenendo wangu unamchukiza ndugu Mkristo? (1)**

_____ Ipuuze. Hakuna mtu anayeweza kumpendeza kila mtu.
_____ Pambana, na mmoja baada ya mwingine.
_____ Jaribu kumfanya ndugu huyo atengwe na ushirika.
_____ Mwambie kila mtu ili washiriki wa kanisa wachague upande.
_____ Acha kufanya jambo la kuudhi.

**16. Yesu anamwitaje mtu ambaye ameazimia kufuata njia yake mwenyewe badala ya kusikiliza shauri la Biblia? (1)**

_____ Mwanafikra huru.
_____ Mtu mwenye busara.
_____Mjinga.

**17. Mtu anayekataa viwango vya Yesu vya maisha ya Kikristo (1)**

_____ Ghafla ataanza kupenda mambo ya kiroho anapofika mbinguni.
_______ Atatubu kwa ajili ya ugumu wa moyo wake baada ya siku chache katika mji mtakatifu.
_____ Ataleta huzuni mbinguni.

**Hakuna kurudi nyuma**

**Somo la 27**

Mrukaji angani yaani Skydiver akiwa angani kisha akatoka nje kwenye mlango wa ndege na kuruka mbali na ndege, huyo anajua hakuna kurudi nyuma. Ameenda mbali sana, na ikiwa atasahau kufunga kamba kwenye parachuti yake, hakuna kitu kinachoweza kumwokoa na hakika atashuka hadi kifo cha kutisha. Ni msiba ulioje huo! Lakini kuna jambo baya zaidi ambalo linaweza kumtokea mtu kuliko hilo. Kwa kweli, ni mbaya zaidi kufikia hatua ya kutorudi katika mahusiano yako na Mungu. Walakini mamilioni wanakaribia hatua hii nao hawajui! Je, Inawezekana kwamba wewe ni mmoja wao? Je! Ni dhambi gani mbaya ambayo inaweza kusababisha hatima kama hiyo? Kwa nini Mungu hawezi kuisamehe? Jibu ambalo ni wazi na lenye kupenya ndani ya akili, lakini pia limejaa matumaini lipo hapa, chukua dakika chache na Mwongozo huu wa kuvutia katika Somo.

1. Je! Ni dhambi gani ambayo Mungu hawezi kusamehe?
" Kwa sababu hiyo nawaambia, Kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho hawatasamehewa.." Mathayo 12:31.

**Jibu:** Dhambi ambayo Mungu hawezi kusamehe ni "kumkufuru Roho Mtakatifu." Lakini ni nini maana ya "kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu"? Watu wana imani tofauti kuhusiana na dhambi hii. Wengine wanaamini ni mauaji; wengine, kumlaani Roho Mtakatifu; wengine, kujiua; wengine, kuua mtoto ambaye hajazaliwa; wengine, kumkana Kristo; wengine, kitendo kibaya cha kutisha, na kiovu mno; na wengine, kuabudu mungu wa uwongo! Swali lifuatalo litatoa mwanga kuhusu jambo hili muhimu.

Mauaji, ingawa ni mabaya, sio dhambi ambayo Mungu hawezi kusamehe. Kuna watu kwenye Biblia waliua na watakwenda mbinguni. Hii isitufanye tusiue! Mmojawapo ni Musa, na Daudi

2. Je! Biblia inasema nini juu ya dhambi ya kukufuru?
"Kwa sababu hiyo nawaambia, Kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho hawatasamehewa. [32] Naye mtu ye yote atakayenena neno juu ya Mwana wa Adamu atasamehewa, bali yeye atakayenena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao.." Mathayo 12:31.

**Jibu:** Biblia inasema wazi kwamba kila aina ya dhambi na kufuru zitasamehewa. Kwa hivyo hakuna dhambi iliyoorodheshwa katika swali lililopita ambayo Mungu hawezi kuisamehe. Hakuna *tendo moja* la aina yoyote ile ambayo linafanya dhambi isiyosameheka.

**Sauti Zinazokinzana**
Ndio, inaonekana kupingana, lakini taarifa zote mbili zifuatazo ni za kweli:

A. Dhambi za kila aina za dhambi na kukufuru zitasamehewa.

B. Kumkufuru au kumtendea dhambi Roho Mtakatifu hakutasamehewa.

Yesu Alitoa Kauli Zote Hizo

Yesu alitoa taarifa zote mbili katika Mathayo 12:31, kwa hivyo hakuna kosa hapa. Kwa kuoanisha taarifa lazima tugundue kazi ya Roho Mtakatifu. Kwa njia, neno "mzimu" linatokana na "ghost", neno la Kiingereza la Kale la "roho".

Roho Mtakatifu huwaongoza watu kwenye Ukweli wa Biblia.

3. Kazi ya Roho Mtakatifu, au Roho ni nini?

"Yeye [Roho Mtakatifu] atauhukumu ulimwengu juu ya dhambi, na haki, na hukumu." "Atakuongoza katika ukweli wote." Yohana 16: 8, 13, NKJV.

**Jibu:** Kazi ya Roho Mtakatifu ni kunithibitisha juu ya dhambi na kuniongoza katika Kweli yote. Roho Mtakatifu ni wakala wa Mungu wa uongofu. Bila Roho Mtakatifu, hakuna mtu anayehisi huzuni au majutokwa ajili ya dhambi, na hakuna mtu aliyewahi kuongoka bila Roho Mtakatifu.

Mungu atasamehe dhambi yoyote ambayo ninakiri Kwake.

4. Wakati Roho Mtakatifu ananihakikishia dhambi, ni lazima nifanye nini ili nisamehewe?

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atusamehe dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yohana 1: 9.

**Jibu:** Ninapohukumiwa dhambi na Roho Mtakatifu, lazima nikiri dhambi zangu ili nisamehewe. Ninapokiri, Mungu hunisamehe lakini pia hunisafisha kimiujiza kutoka kwa udhalimu wote. Mungu anasubiri na Yuko tayari kunisamehe kwa dhambi yoyote ambayo nimewahi kufanya (Zaburi 86: 5), lakini endapo tu nitakiri na kuiacha.

Wale wanaoficha dhambi badala ya kuikiri hawatabarikiwa na Mungu.

5. Je, ni nini kinachotokea ikiwa situbu dhambi zangu japo nimesadikiswa na Roho Mtakatifu?

"Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema." Mithali 28:13.

**Jibu:** Ikiwa sikiri dhambi zangu, Yesu hawezi kunisamehe dhambi zangu. Kwa hivyo, dhambi yoyote ambayo sikiri haiwezi kusamehewa mpaka nikiungama, kwa sababu msamaha kila wakati hufuatia ungamo. Halitangulii ungamo kamwe!

**Hatari ya Kutisha ya kumpinga Roho Mtakatifu**

Kumpinga Roho Mtakatifu ni hatari sana kwa sababu husababisha urahisi kumkataa Roho Mtakatifu, ambayo ni dhambi ambayo Mungu hawezi kusamehe kamwe. Ni kupita hatua ya kurudi. Kwa kuwa Roho Mtakatifu ndiye chombo pekee kilichopewa kuniletea kusadikika, ikiwa nitamkataa kabisa, kesi yangu haina tumaini baadaye. Somo hili ni muhimu sana kwamba Mungu anaelezea na kuelezea njia nyingi tofauti katika Maandiko. Tazama maelezo haya tofauti unapoendelea kuchunguza Mwongozo huu wa Somo.

Ninapohukumiwa dhambi na Roho Mtakatifu, lazima nijibu mara moja.

6. Wakati Roho Mtakatifu ananihukumu juu ya dhambi au ananielekeza kwenye Ukweli mpya, ni nini mimi napaswa kutenda?

**Jibu:** Biblia inasema:

A. "Mara tu watakaponisikia juu yangu, watanitii." Zaburi 18:44.

B. "Nilifanya haraka, wala sikucheleweshа kuzishika amri Zako." Zaburi 119: 60.

C. "Tazama, sasa ni wakati unaokubalika tazama, sasa ni siku ya wokovu." 2 Wakorintho 6: 2.

D. "." Matendo 22:16.

Biblia inasema mara kwa mara kwamba ninapopatikana na hatia ya dhambi, lazima nikiri mara moja na kutubu. Na ninapojifunza Ukweli mpya, lazima niupokee bila kuchelewa.

Mungu aliwaonya watu katika siku za Nuhu kwamba Roho Wake Mtakatifu hataendelea kuwasihi milele; hata leo ni vile vile.

7. Ni maonyo gani mazito anayotoa Mungu juu ya kusihi kwa Roho Wake Mtakatifu?
"Roho Yangu haitashindana na mwanadamu kila wakati." Mwanzo 6: 3.

**Jibu:** Mungu anaonya kabisa kwamba Roho Mtakatifu haendelei kumwomba mtu aachane na dhambi na kumtii Mungu.
Kuzima kengele/alarm ya saa inapokuamsha na kuiweka chumba kingine, humleta mtu mahali ambapo hawezi kuusikia mlio huo tena. Vivyo hivyo, kumfungia nje Roho Mtakatifu kunasababisha kuwa kiziwi kwa sauti Yake.

8. Je! Ni wakati gani Roho Mtakatifu anaacha kumsihi mtu?
"Kwa hiyo nasema nao kwa mifano: kwa sababu ... wakisikia hawasikii." Mathayo 13:13.

**Jibu:** Roho Mtakatifu huacha kuzungumza na mtu wakati mtu huyo atakuwa kiziwi kwa sauti Yake. Biblia inaelezea kama kusikia, lakini sio kusikia. Hakuna maana kuweka kengele kwenye saa katika chumba cha mtu kiziwi. Yeye hatasikia. Kusikia hapa ni kuyaweka maneno haya moyo nina akilini na kuyatenda, na si masikio mawili uliyo nayo kichwanimwako. Vivyo hivyo, mtu anaweza kujipangia katika maisha yake asisikie kengele ya saa kwa kuizima mara kwa mara na kutokuinuka. Mwishowe itakuja siku wakati kengele inalia naye hasikii.

**<u>Usimfungie Roho Mtakatifu</u>**

Ndivyo ilivyo na Roho Mtakatifu. Ikiwa nitaendelea kumfungia, siku moja atazungumza nami na sitamsikia. Siku hiyo inapofika, Yeye Roho kwa huzuni

ataniacha kwa sababu nimekuwa kiziwi kwa maombi Yake. Nimepitiliza hatua ya kurudi. Hili ni onyo zito, linalotia wasiwasi dhidi ya kuipinga sauti ya Roho! Wakati ninapokea nuru mpya kutoka kwa Neno la Mungu, lazima niifuate mara moja bila kuchelewa.

9. Mungu, kupitia Roho Wake Mtakatifu, huleta nuru (Yohana 1: 9) na kumsadikisha(Yohana 16: 8) kwa kila mtu hapa duniani. Nifanye nini wakati ninapokea nuru kutoka kwa Roho Mtakatifu basi?
"Njia ya mwenye haki ni kama taa iangazayo, inayoangaza zaidi na zaidi hata siku ile kamilifu. Njia ya waovu ni kama giza." Mithali 4:18, 19. "Tembeeni mkiwa na nuru, giza lisije likawashinda." Yohana 12:35.

**Jibu:** Kanuni ya Biblia ni kwamba wakati Roho Mtakatifu ananiletea nuru mpya au kunisadikika kwa dhambi, lazima nitende mara moja - Nitii bila ya kuchelewa. Ikiwa nitatii na kutembea katika nuru kama ninavyoipokea, Mungu ataendelea kunipa nuru. Nikikataa, hata nuru niliyo nayo itazimwa, nami nitabaki gizani. Giza linalotokana na kukataa kuendelea kufuatilia mpaka mwisho kuifuata nuru ni matokeo ya kumkataa Roho, na hali hiyo itaniacha mimi bila matumaini.
Dhambi isiyosameheka ya Yuda ilikuwa tamaa kwa sababu alikataa kukiri na kuiacha.

10. Je! Kuna dhambi yoyote inayoweza kuwa dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu?
**Jibu:** Ndio, ikiwa nitakataa kabisa kukiri na kuacha dhambi yoyote, mwishowe nitakuwa kiziwi kwa Roho Mtakatifu na hivyo kufikia hatua ya kupitiliza na kushindwa kurudi. Ifuatayo ni mifano michache ya Biblia:

A. Dhambi ya Yuda Iskariote isiyosameheka ilikuwa ni uchoyo, yaani tamaa na ubinafsi (Yohana 12: 6). Kwa nini? Je! Ni kwa sababu Mungu hakuweza kusamehe? Hapana! Haikusameheka tu kwa sababu Yuda alikataa kumsikiliza Roho Mtakatifu na kukiri dhambi yake ya kutamani. Mwishowe akawa kiziwi kwa sauti ya Roho.

B. Dhambi isiyosameheka za Lusifa ilikuwa kiburi na kujikweza (Isaya 14: 12-14). Mungu anaweza kusamehe dhambi hizi zote. Lusifa angeweza kusamehewa na kusafishwa, lakini alikataa kusikiliza mpaka ikafikia hatua ambayo asingeweza tena kusikia sauti ya Roho.

C. Dhambi isiyosameheka ya Mafarisayo ilikuwa kukataa kumkubali Yesu kama Masihi (Marko 3: 22-30). Waliaminishwa mara kwa mara na usadikisho wa kina kutoka moyoni kwamba Yesu alikuwa Masihi, Mwana wa Mungu aliye hai wa mbinguni. Lakini waliifanya mioyo yao kuwa migumu na kwa ukaidi walikataa kumpokea kama Mwokozi na Bwana. Mwishowe wakawa viziwi kwa sauti ya Roho. Basi siku moja, baada ya muujiza mwingine mkuu wa Yesu, Mafarisayo waliuambia umati kwamba Yesu alipokea nguvu Zake kutoka kwa shetani.

Kristo mara moja aliwaambia kwamba kuielezea nguvu Yake ya kufanya miujiza inatoka kwa shetani ilionyesha kuwa wamepita hatua ya kurudi Kwake na hivyo wamemkufuru Roho Mtakatifu. Mungu angeweza, na kwa furaha angekuwa

amewasamehe. Lakini walikataa mpaka wakawa viziwi kwa Roho Mtakatifu na hawangeweza kufikiwa tena.

**Siwezi Chagua Matokeo au athari**

Wakati Roho anatoa rufaa yake, ninaweza kuchagua kujibu au kukataa, lakini siwezi kuchagua matokeo. Wao ni yamekuwa, hayawezi kubadilika. Ikiwa nitajibu kila wakati kuwa upande wa Bwana, nitakuwa kama Yesu. Roho Mtakatifu atanitia muhuri, au kunitia alama katika paji la uso kama mtoto wa Mungu (Ufunuo 7: 2, 3), na hivyo kunihakikishia nafasi katika ufalme wa Mungu wa mbinguni. Ikiwa nitakataa kujibu mwito Wake, nitamhuzunisha Roho Mtakatifu Naye ataniacha milele, na hivyo kuifunga adhabu yangu. Ni Onyo kali kama nini kupuuza Roho Mtakatifu!

Mfalme Daudi alijua kwamba ikiwa Roho Mtakatifu atamwacha, yeye atapotea. Ndio maana alimwomba Mungu asimwondoe Roho Wake Mtakatifu.

**11. Baada ya Mfalme Daudi kufanya dhambi mbili mbaya za uzinzi na mauaji, Je, aliomba sala gani yenye uchungu?**

" . Usinitenge na uso wako, Wala Roho Wako mtakatifu asiniondolee.." Zaburi 51:11.

**Jibu:** Alimsihi Mungu asimwondoe Roho Mtakatifu kutoka kwake. Kwa nini? Kwa sababu Daudi alijua ikiwa Roho Mtakatifu atamwacha, atakuwa amepotea tangu wakati huo. Alijua kwamba ni Roho Mtakatifu tu Ndiye anayeweza kumpeleka kwenye toba na urejesho, na alitetemeka kwa wazo la Roho kuwa kiziwi kwa sauti yake. Biblia inatuambia mahali pengine kwamba mwishowe Mungu alimwacha Efraimu peke yake kwa sababu alikuwa amejiunga na sanamu zake (Hosea 4:17) na hangemsikiliza Roho. Alikuwa kiziwi kiroho. Jambo la kusikitisha zaidi ambalo linaweza kumtokea mtu yeyote ni kwa Mungu lazima ageuke na kumwacha peke yake. Usikubali kutokea kwako!

Dhambi ni kama maji. Kuendelea katika dhambi huzima moto wa Roho Mtakatifu.

**12. Paulo alitoa amri gani zito na nzito kwa kanisa la Thesalonike?**

"Msimzimishe Roho." 1 Wathesalonike 5:19 .

**Jibu:** Kusihi kwa Roho Mtakatifu ni kama moto unaowaka katika akili na moyo wa mtu. Dhambi ina athari sawa kwa Roho Mtakatifu kama vile maji yalivyo kwa moto unaowaka. Ninapompuuza Roho Mtakatifu na kuendelea katika dhambi, ninamimina maji kwenye moto wa Roho Mtakatifu. Maneno yenye kustaajabisha ya Paulo kwa Wathesalonike yanatuhusu sisi leo. Usizime moto wa Roho Mtakatifu kwa kukataa mara kwa mara kutii sauti ya Roho. Ikiwa moto utazima, nimepita hatua ya kurudi.

**Dhambi Yoyote Inaweza Kuzima Moto**

Dhambi yoyote ambayo haijaungamwa au ambayo haijaachwa inaweza hatimaye kuzima moto wa Roho Mtakatifu. Inaweza kuwa kukataa kushika Sabato takatifu ya Mungu ya siku ya saba. Inaweza kuwa matumizi ya tumbaku. Inaweza kuwa kushindwa kumsamehe mtu ambaye amekusaliti au kukuumiza kwa njia nyingine.

Inaweza kuwa uasherati. Inaweza kuwa ni kujichukulia fungu la kumi la Mungu. Kukataa kutii sauti ya Roho Mtakatifu katika eneo lolote kunamimina maji kwenye moto wa Roho Mtakatifu. Usizime moto. Hakuna msiba mkubwa zaidi unaoweza kutokea kama huu.

**13. Ni kauli gani nyingine ya kushtua, isiyoweza kufikirika ambayo Paulo aliwaambia waamini wa Thesalonike?**
"na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea, kwa sababu hawakukubali kuipenda ile Kweli wapate kuokolewa. Na kwa ajili hiyo Mungu atawaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo; wahukumiwe wasioiamini Kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu." 2 Wathesalonike 2:10-12 .

**Jibu:** Maneno yenye nguvu jinsi gani haya na ya kushtua! Mungu anasema kwamba wale wanaokataa kupokea Ukweli na usadikisho unaoletwa na Roho Mtakatifu watapata (baada ya Roho kuwaacha) watapokea upotofu mkubwa wa kuamini kwamba kosa ni kweli. Ongea juu ya wazo la kutisha!
Bwana atawafunga wengi wanaojiita Wakristo kutoka mbinguni kwa sababu wanakataa kumtii.

**14. Ni jambo gani la kuhuzunisha kiasi gani ambalo baadhi ya watu ambao wametumiwa udanganyifu huo wenye nguvu watapata katika siku ya hukumu?**
Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa Jina Lako, na kwa Jina Lako kutoa pepo, na kwa Jina Lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia, Sijawahi kuwajua ninyi kamwe: ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Mathayo 7:22 , 23 .

**Jibu:** Wale wanaolia "Bwana, Bwana" watashtuka na kupigwa na butwaa kwa kuwa wamefungiwa nje. Watakuwa na hakika kabisa kwamba wameokolewa. Yesu basi bila shaka atawakumbusha juu ya wakati huo muhimu katika maisha yao ambapo Roho Mtakatifu alileta Ukweli mpya na usadikisho. Jambo lilikuwa wazi kabisa na ni Kweli. Liliwaweka macho usiku kucha, wakiwa na wasiwasi na kushindana juu ya uamuzi. Jinsi mioyo yao ilivyowaka ndani yao kwamba wasikilize na kufuata jambo hilo! Hatimaye katika hali ambayo walisema, "Hapana!" Na walikataa kumsikiliza zaidi Roho Mtakatifu. Kisha ukaja upotofu mkubwa uliowafanya wajisikie wameokoka walipopotea. Je, mwanadamu anaweza kukabili msiba mkubwa zaidi?
Uhakikisho wa kutomtii Mungu ni uhakikisho wa uwongo ambao utawaangamiza wengi.

**15. Ni maneno gani ya pekee ya onyo ambayo Yesu anatoa ili kutusaidia tuepuke kuamini kwamba tumeokolewa wakati kiukweli tumepotea?**
"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni." Mathayo 7:21 .
**Jibu:** Yesu alionya kwa dhati kwamba si wote walio na uhakika mioyoni mwao wataingia katika ufalme Wake, bali ni wale tu wanaofanya mapenzi Yake. Sisi sote tunatamani uhakikisho wa wokovu. Ni sharti la mbingu. Hata hivyo, kuna uhakikisho wa uwongo unaoenea sana katika Jumuiya ya Wakristo leo ambao huwaahidi watu

wokovu huku wakiendelea kuishi katika dhambi na kutoonyesha mtindo wowote wa maisha uliobadilika au hata kujisalimisha kwa maagizo Yake Bwana.

**Wachungaji Wamechanganyikiwa**

Viongozi wa kanisa mashuhuri katika makanisa ambayo yamejaa watu ambao wana hisia ya "uhakikisho", lakini kwa kweli hawajabadilishwa na Yesu Kristo. Wala hawamtii Yeye.

**Yesu Aweka mambo wazi kabisa**

Yesu anasema kwamba uhakikisho wa kweli ni kwa wale tu wanaofanya mapenzi ya Baba yake. Ninapomkubali Yesu kuwa Bwana na Mtawala wa maisha yangu, mtindo wangu wa maisha utabadilika sana. Nitakuwa kiumbe kipya kabisa ( 2 Wakorintho 5:17 ). Nitazishika amri Zake kwa furaha, kufanya mapenzi Yake ( Yohana 14:15 ), na kufuata kwa furaha anakoniongoza ( 1 Petro 2:21 ). Nitasema nipeleke popote unapotaka, bora nikufuate. Nguvu Zake za ajabu za ufufuo ( Wafilipi 3:10 ) hunibadilisha kuwa mfano Wake ( 2 Wakorintho 3:18 ). Amani Yake tukufu hufurika maishani mwangu ( Yohana 14:27 ). Yesu akikaa ndani yangu kwa njia ya Roho Wake ( Waefeso 3:16 , 17 ), "Nayaweza mambo yote" ( Wafilipi 4:13 ) na "hakuna lisilowezekana" ( Mathayo 17:20 ).

**Uhakikisho wa Kweli wa Kustaajabisha dhidi ya Uhakikisho wa Bandia**

Ninapofuata Mwokozi anaponiongoza, anaahidi kwamba hakuna mtu awezaye kunitoa mkononi Mwake ( Yohana 10:28 ) na kwamba taji ya uzima inaningoja ( Ufunuo 2:10 ). Ni usalama wa ajabu kiasi gani, wa utukufu, wa kweli ambao Yesu anawapa wafuasi Wake! Uhakikisho ulioahidiwa chini ya masharti mengine yoyote ni ghushi. Itawaongoza watu kwenye upande mbaya wa wa hukumu ya mbinguni, wakihisi kuwa wameokolewa wakati wao, kwa kweli, wamepotea ( Mithali 16:25 ). Nikimfanya Yesu kuwa Bwana wa maisha yangu, anaahidi kuniokoa katika ufalme Wake.

**16. Ni ahadi gani iliyobarikiwa ya Mungu kwa wafuasi Wake waaminifu wanaomtawaza kuwa Bwana wa maisha yao?**

"Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu." "Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kunia na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema." Wafilipi 1:6 ; 2:13 .

**Jibu:** Mungu asifiwe! Wale wanaomfanya Yesu kuwa Bwana na Mtawala wa maisha yao wameahidiwa miujiza ya Yesu ambayo itawafikisha salama hadi kwenye ufalme Wake wa milele. Hakuna kinachoweza kuwa bora zaidi kuliko hicho!
Yesu anaahidi kuingia katika maisha yangu nitakapomfungulia mlango.

**17. Ni ahadi gani ya ziada tukufu ambayo Yesu anatutolea sisi sote?**

"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami." Ufunuo 3:20 .

**Jibu:** Yesu anaahidi kuingia katika maisha yetu tunapomfungulia mlango. Ni Yesu

Ndiye ambaye anabisha mlango wa moyo wako na wangu kwa njia ya Roho Wake Mtakatifu. Yeye—Mfalme wa wafalme, Mwokozi wa ulimwengu—huchukua muda kutoka kwa kuusimamia ulimwengu kuja kwako na kwangu kwa ziara za mara kwa mara za upendo na mwongozo wa kirafiki, kujali na ushauri. Ni upumbavu ulioje, na msiba usioaweza kufikirika, kwamba tutajidai kuwa na shughuli nyingi sana au kutomfurahia na kuwa rafiki na mchangamfu kwake, au kuwa na upendo wa kudumu pamoja na Yesu. Marafiki wa karibu wa Yesu hawatakuwa katika hatari ya kukataliwa siku ya hukumu. Yesu Mwenyewe atawakaribisha katika ufalme Wake ( Mathayo 25:34 ).
Panga kuwa sehemu ya kundi hilo la furaha litakalokutana mawinguni siku ya kutokea Kwake.

**18. Je, utaamua kufungua mlango kila wakati Yesu anapobisha hodi moyoni mwako na kuwa tayari kufuata anakokuongoza?**

**<u>Neno la Kuagana</u>**
Huu ndio Mwongozo wa mwisho wa Mafunzo katika mfululizo wetu wa 27. Hamu yetu ni kwamba wewe umeongozwa katika uwepo wa Yesu na kuwa na uzoefu wa uhusiano mpya wa ajabu Naye. Tunatumai kwamba utatembea karibu na Bwana kila siku na hivi karibuni utajiunga na kundi hilo la furaha ambalo litachukuliwa katika ufalme Wake uliobarikiwa wakati wa kutokea Kwake. Tusipokutana hapa duniani, tukubaliane kukutana mawinguni siku hiyo kuu.

**Maswali ya Mawazo**

**1. Biblia inasema kwamba Mungu aliufanya moyo wa Farao kuwa mgumu (Kutoka 9:12). Hiyo haionekani kuwa sawa. Ina maana gani?**
Roho Mtakatifu huwasihi watu wote ( Yohana 1:9 ), kama vile jua huangaza kila mtu na kila kitu. Jua lile lile linalofanya udongo kuwa mgumu pia huyeyusha nta. Roho Mtakatifu pia ana athari tofauti juu ya mioyo yetu kulingana na jinsi tunavyohusiana na kusihi Kwake. Nikiitikia, moyo wangu utalainishwa na nitabadilishwa kabisa

( 1 Samweli 10:6 ). Nikimpinga Roho, moyo wangu utakuwa mgumu ( Zekaria 7:12 ).

**<u>Jibu la Farao</u>**
Farao aliufanya moyo wake kuwa mgumu kwa kumpinga Roho Mtakatifu ( Kutoka 8:15 , 32 ) 9:34 ). Lakini Biblia pia inazungumza kuhusu Mungu kuufanya moyo wake kuwa mgumu kwa sababu Roho Mtakatifu wa Mungu aliendelea kumsihi Farao. Kwa kuwa Farao aliendelea kupinga, moyo wake ukawa mgumu kama vile jua linavyofanya udongo kuwa mgumu. Ikiwa Farao angesikiliza, moyo wake ungekuwa laini kama vile jua linavyolainisha nta ya sega la asali.

**<u>Yuda na Petro</u>**
wanafunzi wa Kristo Yuda na Petro walionyesha kanuni hiyohiyo. Wote wawili walikuwa wametenda dhambi nzito. Mmoja alimsaliti na mwingine akamkana Yesu. Ipi ni mbaya zaidi? Nani anaweza kusema? Roho Mtakatifu Yule Yule mchangamfu aliwasihi wote wawili. Yuda akafanya moyo wa chuma, na moyo wake ukawa kama

jiwe. Petro, kwa upande mwingine, alikuwa msikivu kwa Roho Mtakatifu na moyo wake ukayeyuka. Alitubu kweli na baadaye akawa mmoja wa wahubiri wakuu katika kanisa la mitume. Tafadhali soma Zekaria 7:12 , 13 ili upate onyo zuri la Mungu kuhusu kuifanya mioyo yetu kuwa migumu dhidi ya kusikia na kutii maombi ya Roho Wake.

**2. Unafikiri nini kuhusu kuomba "ishara" kutoka kwa Bwana?**
Katika Agano Jipya, Yesu anazungumza kwa uamuzi dhidi Yake. Alisema, "Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara." Mathayo 12:39 . Alikuwa akifundisha Ukweli na kuuunga mkono kutoka katika Agano la Kale, ambalo lilikuwa Maandiko yaliyopatikana wakati huo. Walielewa vizuri sana kile alichokuwa akisema. Pia waliona miujiza yake, lakini bado walimkataa. Baadaye alisema, "Kama hawawasikii Musa na manabii, hawatashawishwa hata kama mmoja atafufuka kutoka kwa wafu. Luka 16:31 . Biblia inatuambia tujaribu kila kitu kwa Maandiko ( Isaya 8:19 , 20 ). Ikiwa tunajitolea kufanya mapenzi ya Yesu na kufuata anakotuongoza, anaahidi kwamba atatusaidia kutambua Ukweli kutoka kwa makosa ( Yohana 7:17 ).

**3. Je, kuna wakati ambapo maombi hayasaidii?**
Ndiyo. Ikiwa mtu anakosa kumtii Mungu kwa kujua ( Zaburi 66:18 ) na bado anamwomba Mungu ambariki (ingawa hana mpango wa kubadilika), sala ya mtu huyo si tu kwamba haina thamani, bali Mungu husema ni chukizo ( Mithali 28:9 ) . .

**4. Nina wasiwasi sana kwamba huenda nimemkataa Roho Mtakatifu na siwezi kusamehewa. Unaweza kunisaidia?**
Hujamkataa Roho Mtakatifu. Unaweza kujua hilo kwa sababu unahisi wasiwasi au hatia. Ni Roho Mtakatifu pekee Ndiye anayekuletea wasiwasi na usadikisho ( Yohana 16:8-13 ). Ikiwa Roho Mtakatifu angekuacha, kusingekuwa na wasiwasi au usadikisho ndani ya moyo wako. Furahi na kumsifu Mungu! Mpe maisha yako sasa! Na kwa maombi mfuate na kumtii katika siku zijazo. Yeye Atakupa ushindi ( 1 Wakorintho 15:57 ), atakutegemeza ( Wafilipi 2:13 ), na kukuweka mpaka ujio Wake wa pili ( Wafilipi 1:6 ).

**5. Katika mfano wa mpanzi ( Luka 8:5-18 ), ni nini maana ya mbegu iliyoanguka kando ya njia na kuliwa na ndege?**
Biblia inasema, "Mbegu ni Neno la Mungu. Wale wa kando ya njia ni wale wanaosikia, kisha huja Ibilisi na kuliondoa Neno hilo mioyoni mwao, wasije wakaamini na kuokolewa." Luka 8:11 , 12 . Yesu anaashiria kwamba tunapoelewa kile ambacho Roho Mtakatifu anatutaka tufanye kuhusu nuru mpya kutoka kwa Maandiko, lazima tuchukue hatua mara moja. Vinginevyo, shetani ana nafasi ya kuondoa Ukweli huo kutoka kwa akili zetu.

**6. Je! Bwana anawezaje kusema "sikuwajua ninyi kamwe" kwa watu anaowahutubia katika Mathayo 7:21-23? Nilidhani Mungu alijua kila mtu na kila kitu!**
Mungu anarejelea hapa kumjua mtu kama rafiki wa kibinafsi/mwandani. Tunapata kumjua Yeye kama rafiki tunapowasiliana Naye kila siku, kumfuata kwa furaha, na kushiriki Naye kwa hiari furaha na huzuni zetu kama na rafiki wa duniani. Yesu

pia anasema, “Ninyi mmekuwa rafiki Zangu, mkitenda niwaamuruyo.” Yohana 15:14 . Watu wanaozungumziwa katika Mathayo sura ya 7 wamemkataa Roho Wake Mtakatifu. Wameikubali theolojia ya wokovu katika dhambi au wokovu kwa matendo--ambayo yote hayo hayamhitaji Yesu. Ni watu waliojitengeneza wenyewe ambao hawakuchukua muda kumfahamu Yesu. Kwa hiyo, Yeye aeleza kwamba hakuwapata kuwafahamu au kuwajua kuwa marafiki Zake wa kibinafsi.

**7. Je, unaweza kueleza Waefeso 4:30?**

Mstari huo unasema, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa Yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi.” Paulo hapa anadokeza waziwazi kwamba Roho Mtakatifu ni kiumbe binafsi, kwa sababu ni watu pekee wanaoweza kuhuzunishwa. Hata muhimu zaidi, anathibitisha kwamba Roho Mtakatifu wa Kristo anaweza kuhuzunishwa na kukataa kwangu maombi Yake ya upendo. Kama vile uchumba unavyoweza kukomeshwa milele kwa kukataa mara kwa mara kwa upande mmoja kwa kusihi kwa mwingine, vivyo hivyo uhusiano wetu na Roho Mtakatifu unaweza kuisha kabisa kwa kukataa kwetu kuitikia maombi Yake ya upendo.

**Maswali ya Maswali**

**1. Dhambi yoyote ile inaweza kuwa dhambi ambayo Mungu hawezi kusamehe. (1)**

_____ Ndiyo.

_____ Hapana.

**2. Dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu ni (1)**

_____ Mauaji.

_____ Kumlaani Mungu.

_____ Kumkataa Roho Mtakatifu.

**3. Roho Mtakatifu lazima wakati fulani ajiondoe kwa mwenye dhambi kwa huzuni kwa sababu (1)**

_____ Roho Mtakatifu ana mambo mengine ya kufanya.

_____ Roho Mtakatifu ana hasira ya haki juu ya tabia mbaya ya mwenye dhambi.

_____ Mungu anamwambia afanye jambo lingine.

_____ Mwenye dhambi amekuwa kiziwi kwa kusihi kwake.

**4. Roho Mtakatifu anaweza “kuzimishwa” kwa kuendelea katika dhambi wakati unajua vizuri zaidi. (1)**

_____ Ndiyo.

_____ Hapana.

**5. Dhambi au kufuru yoyote itasamehewa ikiwa (1)**

_____ Nitaomba vya kutosha kuhusu hilo.

_____ Kiri kwa Yesu kwa dhati.

_____ Funga kwa siku kadhaa.

_____ Nitakuwa Shahidi kwa uaminifu.

**6. Bila Roho Mtakatifu, hakuna mtu anayehuzunika kwa ajili ya dhambi, wala hakuna aliyeongoka. (1)**
_____ Kweli.
_____ Uongo.

**7. Uhakikisho wa wokovu wakati mwingine unaweza kuwa bandia. Baadhi ya watu ambao wana hakika wameokoka wamepotea. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**8. Angalia vitu ambavyo ni kazi ya Roho Mtakatifu kulingana na Yohana 16:8, 13: (2)**
_____ Nifundishe jinsi ya kuimba.
_____ Nipe karama ya unabii.
_____ Nifanye niwe na furaha.
_____ Nitie hatiani juu ya dhambi.
_____ Niongoze kwa Ukweli.

**9. Roho Mtakatifu anaponitia hatiani kuhusu zile Kweli mpya au kunionyesha dhambi maishani mwangu, ni lazima (1)**
_____ Kuuliza mchungaji kuhusu hilo.
_____ Nenda ukamwone mwanasaikolojia.
_____ Mwombe Mungu ishara.
_____ Fuata mwongozo wa Roho bila kusita.
_____ Geuza sarafu.

**10. Kwa nini Daudi alimsihi Mungu asimwondoe Roho Mtakatifu? (1)**
_____ Kwa sababu Roho Mtakatifu alimsaidia kupiga kinubi chake.
_____ Kwa sababu aliogopa kwamba Roho Mtakatifu anaweza kuchukua maisha yake.
_____ Kwa sababu alijua angekuwa mtu aliyepotea ikiwa Roho angeondoka kwake.

**11. Kulingana na Mathayo 7:21-23, kwa mtu kufanya miujiza, kutoa pepo, kutabiri kwa jina la Yesu, na kudai Yeye kama Bwana haitatosha siku ya hukumu. Ni nini kingine ambacho Yesu alisema kilikuwa muhimu kabisa? (1)**
_____ Kufanya ushuhuda mwingi.
_____ Kuomba mara kwa mara hadharani.
_____ Kufunga mara kwa mara.
_____ Kuhudhuria kanisa mara kwa mara.
_____ Kufanya mapenzi ya Baba wa mbinguni.

**12. Kulingana na 2 Wathesalonike 2:10-12 , ni nini kitakachowapata wale wanaokataa kupokea Kweli? (1)**
_____ Wataokolewa hata hivyo.
_____ Mungu atawauliza wafikirie upya.
_____ Mungu atawaletea upotovu mkubwa, na wataamini kuwa uwongo ndio ukweli.

**13. Bwana anaposema "Sikuwajua ninyi kamwe" katika hukumu, anamaanisha (1)**
_____ Hajui mtu huyo ni nani.
_____ Uso unajulikana, lakini Amesahau jina.
_____ Mtu huyo hakuwahi kuchukua muda wa kufahamiana Naye kama rafiki wa kibinafsi.

**14. Yesu, katika Agano Jipya, alifundisha dhidi ya kuomba ishara. (1)**
_____ Ndiyo.
_____ Hapana.

**NB; Wengi wamewekamatumaini yao kwa wazazi, ndugu jamaa na marafiki na hata wachungaji. Lakini Neno la Mungu linatuonya kuwa tusiweke matumaini yetu kwa watu maana watu wana udhaifu mwingi. Wapo wachungaji wengi leo wanaojipatia faida binafsi toka kwa waumini wao. Wako tayari hatakutumia mbinu zisizofaa maadam tu wajipatie faida wao binafsi bila kujali washiriki wao. Hii imesababisha manabii wa uongo wanaofanya miujiza bandia ili tu wajipatie pesa.**

**Mpendwa mtafute Mungu wa Kweli hapo utakuwa salama. Bwana hatakawia, dalili zinaonyesha Yeye atarudi hivi karibuni. Nasi tungependa tumfuate Mwana-Kondoo kila tunapokwenda. Biblia inasema kwamba, kwa Bwana siku moja ni miaka elfu moja kwetu, hivyo hata wakina Methuselah, au Adamu walioishi sana waliishi masaa kama 20 hivi, na sisi tukiishi miaka 70 tutakuwa tumeishi masaa 2 tu, hivyo japokuwa tunaona kwamba sisi tuna wadhifa na cheo sana, ukweli ni kwamba utu, wadhifa au cheo chetu tumepewa Naye, Mwenyezi Mungu anayetaka tuishi maisha yanayopimwa kwa urefu sawa na Yake!, yaani milele! Milele ni muda mrefu, na maisha yanakuwa bora tukiamua kuwa kule, maana hakika tutakuwa na furaha ya kweli, nami pia naamini Yale Bwana amesema**

**Tuombeane.**
YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina

Grace Momadi-Masaka na Daniel Masaka,
**Injili Kiswahili Uhamishoni Ughaibuni au Mtandaoni**

---

*Kwa Maswali na Majibu:*
*Simu: +255 -755 -040766*
*Mbeya - Tanzania.*
*Barua pepe: kwelizabiblia@gmail.com*

---

**ASOMAYE NA AFAHAMU**- 1

Masomo haya ya kitabu cha Danieli yameandaliwa kwa kifupi mno; YESU alisema tusome kitabu hiki kwenye Mathayo 24:15. Hakuna kitabu kingine kilichonakiliwa alichosema tukisome, na wakati huu Agano Jipya halikuwepo bado! Mambo machache muhimu yamegusiwa kwa juu juu tu. Kwa maelezo ya fungu kwa fungu itabidi msomaji asome vitabu kama ***Danieli na Siku Zetu, na vingine vya kingereza mfano Daniel na*** Norman McNulty **.** Jaribu kukisoma kwa makini kitabu cha Biblia cha Danieli kwani majibu karibu yote yamo humu! Kuna masomo mengi ya Kingereza na Kiswahili kwenye mtandao pia, mojawapo kwa Kiswahili ni Mchungaji Semba katika masomo ya "UNABII WA KITABU HIKI SEHEMU 1:UHUSIANO KATI YA DANIEL NA UFUNUO na MCHUNGAJI SEMBA.". Kitabu cha Daniel na Ufunuo ni kitabu kimoja tu kuhusiana na mambo yajayo au Apokalipsi, hiyo usiisahau! Kwanini basi tujifunze vitabu hivi? Kila anayekisoma anapata uzoefu tofauti kabisa wa imani, kwani kinaleta kuzibua fahamu na kuleta matengenezo ya maisha na kubadilisha mwelekeo kabisa. Tunaambiwa heri asomaye naye anayesikia haya. Anasema Naja upesi, shika sana ulicho nacho! Vitabu hivi ni king'ora kinachopiga kuamsha usikivu wa kumtafuta Mungu na kujitayarisha kwa siku ya hukumu. Danieli na Ufunuo vimeandikwa vimejadiliwa na vitabu kuandikwa na watu kadhaa, nitakupa orodha hapa ya vile ambavyo vimenisaidia, mfano Mchungaji Ivory Myers na James Rafferty wana masomo ya 'Salvation in Symbols and Signs' yaani wokovu katika njia ya alama na mifano, Biblia inajitafsiri yenyewe. Mfano maji mengi, maji machache nk. Mchungaji Mark Finley ana masomo ya Ufunuo https://youtu.be/Vtt5Nl4pU84, Mchungaji Doug Batchelor amejifunza unabii wa Ufunuo akiwa duniani, kabla hajawa Mkristo nami miaka 30 iliyopita alinibariki kwa masomo yake ya Amazing Facts and Revelation. Mungu ametufungulia mengi na mengine yanaendelea kufunguliwa utashangaa ukichukua muda na kuanza kusoma nawe pia utaweza kuwafundisha wengine kwa usahihi zaidi! Tumepewa vitabu hivi kuweza kukabili hata mateso kwa imani. Hatuwezi kuyajua Maandiko yote, ila tutayajua kwa usahihi zaidi na ukubwa zaidi kutusaidia siku hizi za mwisho kama tutamwomba Mungu atufunulie, kwani amesema "Heri yake mtu anayesoma kitabu hiki chenye maneno ya ujumbe wa kinabii; na heri yao wanaosikia na kushika yaliyoandikwa humu, maana wakati wa mambo haya umekaribia" Ranko Stefanovich ambaye Nimesoma naye, pia ameandika kitabu kuhusu Ufunuo ambacho ni msaada. Msomaji anatakiwa kuomba kwanza ili kupata mwongozo wa Roho Mtakatifu na kisha kusoma kwanza ile Sura inayohusika kutoka katika Biblia ili kupata habari kamili iliyogusiwa katika mfululizo wa masomo haya, ndipo asome somo la Sura hiyo. Kisha atafakari ili kupata picha kamili. Kitabu cha Danieli kinahusu nyakati zetu hizi za mwisho. Kuelewa mambo yaliyo mbele yetu ni muhimu sana, maana ama tutapata uzima wa milele, ama mauti ya milele katika mkabala wetu na matukio hayo yanayokuja. Hivyo si suala dogo kujifunza unabii wa kitabu cha Danieli kwa wote wanaotaka uzima wa milele. Yesu akizungumza na wanafunzi Wake juu ya matukio ya siku za mwisho alisema, "Basi hapo mtakapoliona ***Chukizo la Uharibifu***, lile lililonenwa na Danieli, limesimama mahali Patakatifu (***asomaye na afahamu***)". Mathayo 24:15. Hatari kubwa i mbele yetu! Yesu anataka kila asomaye alifahamu Chukizo hilo la Uharibifu

linalokuja ili atakapoliona akimbie kuokoa maisha yake (Mt. 24:16-22). Chukizo la Uharibifu limetajwa mahali patatu katika kitabu cha Danieli (Dan. 9:26,27; 11:31; 12:11). Lina majina mengi katika kitabu cha Danieli na cha Ufunuo ----- Pembe Ndogo, Mnyama, na kadhalika. Utashangaa kujua kwamba “mnyama” katika lugha ya taaluma ya unabii sio tusi wala kashfa kama wengi wanavyodhani. Maana yake ni “mfalme au ufalme” (Dan.7:17). Biblia inajitafsiri yenyewe! Hivi maana ya “chukizo” ni nini? Soma 2 Wafalme 21:1-11 na Kumbukumbu laTorati 18:9-14. Kumbe! Chukizo ni kuabudu sanamu, kuwaomba wafu, kushughulika na mapepo, uchawi au ushirikina, kuabudu jua na nyota za mbinguni, na kadhalika. Mataifa, yaani, wapagani hufanya mambo hayo. Je! “uharibifu” ni nini? Sio kuharibu vitu, bali ni kuwaangamiza, yaani, kuwaua watu (Dan.8:24,25). Kwa hiyo, Chukizo la Uharibifu ni mamlaka au utawala au ufalme unaoabudu sanamu, unaowaomba wafu, ulio na ushirikina, na, zaidi ya hayo, unaowaangamiza “watakatifu”, yaani, “hao wazishikao Amri [Kumi] za Mungu na Imani ya Yesu (Ufu.14:12; Kut. 20:3-17; Yak. 2:10-12). Paulo analiita “mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu [mwuaji], mpingamizi [au Mpinga Kristo] (2 The. 2:3,4]. Bila kila mtu kumjua huyo, Yesu Kristo hawezi kuja duniani. Tutaendelea kusumbuka na magonjwa, umaskini, na dhiki. Je! si jambo la muhimu kabisa kuijua mamlaka hiyo ili kujua la kufanya kuokoa maisha yetu, si yale ya kimwili, bali ya kiroho ili tupate kuishi milele? (Mt. 10:26-33; Yoh.6:39-40; Ufu.12:11). Kufa au kutokufa si hoja, bali kujiweka tayari kumlaki Yesu Kristo atakapokuja juu ya mawingu ya mbinguni (Ufu. 2:10; Mt. 24:29-31). Mpendwa Msomaji, Je! kwa neema Yake Mungu unataka kuwa tayari kujiunga na watakatifu ulimwenguni kote? Soma Danieli, na ufahamu. Kabla hujaanza kusoma somo, omba ili Mungu akupe Roho Wake atakayekufundisha Kweli yote (Yohana 16:13-15). Mungu na akubariki! Mwinjilisti Moses Mwalumbili.

## ASOMAYE NA AFAHAMU - 2

## JE! CHAKULA KINAWEZA KUATHIRI AKILI YAKO? (SOMA DANIELI 1 YOTE)

Amini usiamini, chakula kinaweza kuathiri akili yako, na afya yako ya kimwili na kiroho. Kwa maelezo zaidi juu ya somo hili la afya soma vitabu vya Afya na Lishe, kama vile ***Afya na Raha*** na ***Uponyaji wa Mungu*** ambamo zimefafanuliwa Kanuni 8 za Afya ----- Lishe bora, Mazoezi ya mwili, Hewa safi, Maji safi na salama, Mwanga wa jua, Pumziko, Kiasi, na Kumwamini Mungu. Ukizifuata utaepukana na magonjwa mengi na kupunguza gharama ya matibabu. Yatabaki magonjwa yanayokuja kwa njia zingine zisizozuilika ambazo kwaajili ya dhambi huwezi ukaepuka. Chakula cha daraja la kwanza ambacho Mungu alimpa mwanadamu kilikuwa cha “kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu” (Mwanzo 1:29). Dhambi ilipoingia ilileta laana sio tu kwa viumbe vyote bali hata kwa ardhi. Kwa hiyo Mungu akamwongezea mwanadamu mboga za majani katika lishe yake ya awali (Mwanzo 3:18). Gharika ilikaa juu ya nchi kwa miezi mitano au siku 150 na kuharibu mimea yote (Mwanzo 7:24). Kwa hiyo Mungu akamwongezea mwanadamu katika lishe yake “nyama” kutoka kwa wanyama safi tu (Mwa. 8:3,4 imebainishwa na Law. 11:1-47; Kum. 14:1-21). Injini ya petroli

hutumia petroli tu; injili ya dizeli ni dizeli tu. Ukitaka gari lako life weka dizeli katika injini ya petroli au petroli katika injini ya dizeli. Mtengenezaji ndiye anayejua gari lake litatumia mafuta gani, sio mtumiaji. Vile vile, Mungu anajua chakula kinachofaa kwa mwili wa mwanadamu, sio mwanadamu kujichagulia chochote kuwa chakula. Wabishi wataharibu injini za magari yao (miili yao). Mungu aliumba wanyama safi na wanyama najisi juma lile la kwanza la uumbaji. Kifo cha Yesu msalabani hakikuwa kwa kusudi la kuwabadilisha wanyama najisi kuwa wanyama safi, bali wanadamu wenye dhambi kuwa watakatifu. Wale wanaotaka kuwa watakatifu watajiepusha kula nyama inayotokanana wanyama najisi; lakini wale wasiotaka utakatifu wataswaga kila kitu kiingie mdomoni, Mungu ameweka wanyama wengine kama pweza, nguruwe na tai kusafisha nchi na mizoga yake, nasi hatuna haja ya kuvila hivyo vitu baada ya fagio kuviweka kwenye mfumo fulani. (Law. 11:41,43,46,47; Kum. 14:1-4). Mungu hamlazimishi mtu, kama vile mtengenezaji wa injini ya gari asivyomlazimisha mtu kutumia mafuta aliyopendekeza. Lakini matokeo mwilini ni ya hakika. Kisa cha Petro katika Matendo 10:9-16 kimetafsiriwa chini yake katika fungu la 25 hadi 29. Hayo yalikuwa ni maono tu, si kitu halisi; hata hivyo Petro alikataa katakata kuchinja na kula wanyama najisi ingawa ni Mungu mwenyewe aliyemwamuru kufanya hivyo mara tatu. Mungu hana kigeugeu; alisemawa nyama najisi wasiliwe, basi, hawawezi kuliwa milele (Mal. 3:6; Zab. 89:34). Watu wanamsingizia bure Petro wanapochinja wanyama najisi na kula; yeye alikataa katakata. Lakini kuna adhabu kwa wale wanaoendelea kula nguruwe, panya, na machukizo yote ya Mataifa (wapagani). Soma Isaya 65:2-6; 66:15-17). Pombe haikuwa sehemu ya kinywaji ambacho Mungu alimpa mwanadamu; maji safi na salama ndicho kinywaji bora kuliko vyote kwa mwanadamu (Mithali 20:1; 23:29- 35). Walevi hawataurithi ufalme wa Mungu (1 Kor. 6:9,10; Gal. 5:21). Kuna wengi wanaosema, "Mimi nakunywa sana, lakini silewi." Tatizo la pombe sio kulewa tu, bali ni zile athari zinazotokana na kunywa pombe ambayo ina sumu mbaya ya alkoholi. Sumu hiyo huathiri vibaya moyo, mishipa ya fahamu, nyama za mwili na kadhalika. Mungu atamharibu mtu ye yote anayeuharibu mwili wake kwa makusudi kwa njia yo yote ile ----- pombe, tumbako, madawa ya kulevya, na kadhalika (1 Kor. 3:16,17) hufanya mawasiliano yetu na Mungu kuwa hafifu. Pia kuna vinywaji vinavyopendwa na watu wengi aina ya 'Cola', Kahawa, na Majani ya Chai ambavyo huidhuru mishipa ya fahamu, ubongo na mwili. Viepukwe.

## ASOMAYE NA AFAHAMU – 3

Hebu sasa na tuwaangalie wale vijana wanne wa Kiebrania, mateka kutoka Yerusalemu, wakiwa katika jiji lile la Babeli mwaka ule wa 606 au 605 K.K. Walikuwa na umri kati ya miaka 18 na 20. Kutokana na hekima yao walichaguliwa kujiunga na vijana wengine wa Babeli katika Chuo cha Kipagani cha Babeli kwa mafunzo ya miaka mitatu. Wakapewa majina ya miungu ya Babeli ----- Danieli akaitwa Belteshaza,Hanania akaitwa Shadraka, Mishaeli akaitwa Meshaki, na Azaria akaitwa Abednego (Dan. 1:6,7). Mfalme akaamuru wale chakula cha mfalme ili wanenepe na kuwa na akili nyingi. Kusudi lake lilikuwa zuri sana. Lakini, je! chakula kile cha mfalme ambacho kilikuwa na nyama najisi, kilikolezwa kwa viungo vingi vinavyodhuru mwili, na huenda kilikuwa na vileo. nacho kingeweza kuleta afya bora na akili safi? (Dan. 1:1-5). Vijana hao wanne wa Kiebrania walikuwa wamelelewa

katika mazingira tofauti. Walifuata kanuni za afya na chakula ambacho Mungu aliwapa wanadamu kula. Walijiepusha na nyama ya aina yo yote ile pamoja na divai (maji matamu ya zabibu) kwa vile wao walikuwa wanadhiri wa Bwana (Hesabu 6:1-5). Kwa hiyo agizo hilo la mfalme kwao likawa mtihani mgumu sana. "Danieli aliazimu moyoni mwake ya kuwa hatajitia unajisi kwa chakula cha mfalme, wala kwa divai aliyokunywa; basi akamwomba yule mkuu wa matowashi ampe ruhusa asijitie unajisi" (Dan. 1:8). Ni ujasiri ulioje! Ombi lake halikuwa rahisi kukubaliwa na msimamizi yule kwa vile angekatwa kichwa kama wangeonekana wamekondeana (Dan. 1:10).

Basi Danieli akamwambia, "Tafadhali ***utujaribu*** sisi watumishi wako ***muda wa siku kumi***; na watupe mtama [nafaka, kokwa, mboga za majani, matunda] tule, na maji tunywe. Kisha nyuso zetu zitazamwe mbele yako, na nyuso za wale vijana wanaokula chakula cha mfalme..." (Dan. 1:13). Akawakubalia ombi hilo. Je! mambo yalikuwaje kiafya baada ya siku zile kumi tu? "Nyuso zao zilikuwa nzuri zaidi [wale wanaohangaika na vipodozi vinavyodhuru afya wangezingatia hilo], na miili yao ilikuwa imenenepa zaidi, ***kuliko*** wale vijana ***wote*** waliokula chakula cha mfalme. Basi yule msimamizi akaiondoa posho yao ya chakula [cha mfalme], na ile divai waliyopewa wanywe, akawapa mtama [nafaka, kokwa, mboga za majani, matunda] tu" (Dan. 1:15,16). Chakula cha matajiri au wafalme tunachokitamani sana hakileti afya mwilini. Chakula rahisi cha mimea, kisichokobolewa au kusindikwa na maji safi na salama ni lishe bora. Kwa akili safi na mwili wenye afya, ulionenepa au ulionawiri kiafya sio kwa ugonjwa, tumia vyakula vya mimea na maji safi na salama, na kufuata Kanuni zile 8 za Afya. Wana sayansi wamegundua kuwa wale wanaokula vyakula vya mimea bila nyama wanaishi maisha marefu sana kuliko wale wanaokula nyama. Waeskimo wanaoishi kwenye theluji ni mfano mzuri kule juu ya Kanada, wao hawana mimea mingi nao huwinda wanyama wa majini na kwenye nchi. Hawa huishi wastani wa miaka 40 tu. Danieli naye aliishi zaidi ya miaka 90 hadi kufikia kipindi cha utawala wa Koreshi (Dan. 1:21; 10:1). Hebu tuwafuatilie vijana wale wanne mwisho wa mafunzo yao ya miaka mitatu. Mfalme Nebukadreza aliwaonaje? "Naye mfalme akazungumza nao; na ***miongoni mwao wote hawakuonekana*** waliokuwa kama Danieli, na Hanania, na Mishaeli, na Azaria... Na katika kila jambo la ***hekima*** na ***ufahamu*** alilowauliza mfalme, ***akawaona kuwa wanafaa mara kumi Zaidi*** ya waganga na wachawi waliokuwa katika ufalme wake" (Dan.1:19,20). Kwa nini tuhangaike sana na suala la afya ya mwili wetu, je! maisha ya kiroho si bora zaidi? "Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na ***afya*** yako [kimwili], kama vile roho yako ifanikiwavyo" (3 Yohana 2). Wahenga walisema, "Akili timamu katika mwili wenye afya." Ni shauri la kuzingatiwa sana. Kanuni ya Biblia ni hii: "Basi, ***mlapo***, ***mnywapo***, au ***mtendapo neno lo lote*** fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu" (1 Kor. 10:31). Tunawajibika kuitunza miili yetu katika hali ya afya nzuri kadiri iwezekanavyo (l Kor. 6:19,20; 1 Pet. 1:18,19; Rum.12:1,2). Suala la afya linahusu wokovu wetu. Mungu anaweza kututumia kama Danieli (Dan. 1:17). Hawa wasingeweza kutumiwa na Bwana kwa mvuto mkubwa kama wangekuwa katika ulafi wa kubugia vyakula vya mfalme! Mungu huwasiliana nasi kupitia ubongo usio na ukungu.

**ASOMAYE NA AFAHAMU - 4**

**MFALME WA AMANI ANAKUJA UPESI SANA** (SOMA DANIELI 2 YOTE)

Hakuna mwanadamu yeyote awezaye kutabiri kwa hakika mambo yatakayokuja baadaye kwa hekima au maarifa yake mwenyewe. Wanajimu [wanaobashirikwa kuangalia nyota], wachawi wanaotazama bao, wasoma viganja, hata wana sayansi wanabahatisha tu, hawawezi kujua kwa hakika mambo ya zamaniau mambo yanayokuja mbele (Dan.2:27,28; Isa. 42:8,9; 46:9,10; 41:21-24; 8:19; Yak. 4:13-16). Ni Mungu peke yake anayejua mambo ya zamani na yale yajayo, Naye anatuambia kabla hayajatokea. Tangu dhambi iingie duniani mawasiliano ya moja kwa moja na Mungu yalikatika; Sasa Yeye anawasiliana nasi kupitia kwa manabii anaowachagua mwenyewe, maombi, asili, na kwa nadra watu wametokewa na malaika au kusikia sauti ikiwaambia kitu cha kufanya. (Isa.59:2; Hes. 12:6). Matukio yote makubwa yanayoleta maafa kwa wanadamu, Yeye anawajulisha manabii Wake (Amosi 3:7). Kuhusu Gharika alimjulisha Nuhu; kuangamizwa kwa Ninawi alimjulisha Yona; kuangamizwa kwa Sodoma na Gomora alimjulisha Ibrahimu. Mbele yetu kuna mapigo saba (Ufunuo16) ambayo yatawaathiri sana wanadamu. Kabla hayajaja alimjulisha Yohana kisiwani Patmo. Maafa yaliyotiishiwa yanaweza kuepukwa kama watu wanaohusika watatubu na kuacha dhambi zao (Yer. 18:7-10; Yona 3:1-10). Tukiwakataa manabii wanaotumwa na Mungu hatutafanikiwa katika safari yetu ya mbinguni (2 Nya. 20:20). Japo vitabu vya Biblia vilifungwa (Vitabu 66 - Agano la Kale 39; Agano Jipya 27), bado manabii wataendelea kutumwa na Mungu kulionya kanisa lake (Yoeli 2:28-31; Efe.4:11-14). Kwa kuwa wako manabii wa uongo, basi, yatupasa kuwapima. Viko vipimo vinne ambayo nabii ni lazima atimize vyote kuweza kukubalika kama nabii wa kweli wa Mungu ----- 1. Yer. 28:9; Kum. 13:1-5; 2. Isa. 8:20 [Kut.20:3- 17]; 3. Mt. 7:20; 4. 1 Yoh. 4:1-3).

***Unabii*** na ***Historia*** vinakwenda bega kwa bega (Yohana 14:29). Tafsiri sahihi ya unabii itaungwa mkono na mafungu ya Biblia na Historia (Isa. 28:10; 2 Pet. 1:19-21). Unabii hautafsiriwi kama mtu apendavyo au kama kanisa fulani lipendavyo. Ndoto aliyoota mfalme iliyomfadhaisha sana ilihusu Falme Kuu Nne zilizotawala dunia na Falme zilizofuata hadi kuja kwa Yesu Kristo kuja kusimamisha ufalme wake wa milele. Tafsiri ni hii:-

I. UFALME WA BABELI (606-538 au 605-539 K.K.).
Umewakilishwa na ***Kichwa cha dhahabu*** (Dan. 2:37-38). Historia inaunga mkono.

II. UFALME WA WAMEDI NA WAAJEMI (538-331 au 539-331 K.K.).
UliuangushaUfalme wa Babeli (Dan.5:25-31). Unawakilishwa na ***Kifua na Mikono ya Fedha*** (Dan. 2:32a,39a). Historia inaunga mkono. Miaka ni ya kukadiria tu.

III. UFALME WA WAYUNANI (331-168 K.K.)
Ufalme wa Wamedi na Waajemi ulitabiriwa kuwa utaangushwa na Wayunani (Dan. 8:4-7,20-21; 11:1-3). Ufalme wa Wayunani (Wagiriki) unawakilishwa na

***Tumbo naViuno vya Shaba*** (Dan. 2:32b, 39b). Historia inaunga mkono.

**IV. UFALME WA WARUMI (168 K.K. - 476 B.K.).**
Ufalme wa Warumi unawakilishwa na ***Miguu ya Chuma***. Biblia inaielezea vizuri Dola ya Warumi kuwa ilikuwa inazivunja-vunja falme zile nyingine kama chuma. Danieli hakujulishwa jina la Dola hii. Lakini historia inathibitisha kuwa Warumi waliwashinda Wayunani mwaka ule wa 168 K.K. Wakati Kristo anazaliwa Dola hiyo ilikuwa bado inatawala dunia pamoja na Palestina chini ya Kaisari Augusto (Luka 2:1-7; Yohana 11:48).

**ASOMAYE NA AFAHAMU - 5**

V. UFALME WA PAPA (538-1798 B.K.) Ulitokea katika mabaki ya Dola ya Warumi baada ya kuangushwa na makabila ya kishenzi [kipagani] ya Ulaya Kaskazini mwaka wa 476 B.K. Unawakilishwa na ***Nyayo za miguu*** (Dan.2:33b, 41a). Udongo unawakilisha kanisa au watu wa Mungu (Isa.64:8; Yer. 18:6). Chuma kinawakilisha serikali. Hivyo kuchanganyika kwa udongo na chuma ni muungano wa dini na serikali chini ya kiongozi mmoja wa kidini wa Roma. Historia inathibitisha kwamba ufalme huu uliinuka katika mabaki ya Dola ya Warumi baada ya kuangushwa na kutawala dunia kuanzia 538 B.K. Huu ni Utawala wa Papa au Upapa.

VI. FALME KUMI ZA ULAYA MAGHARIBI (476-MAREJEO YA KRISTO)
Falme kumi za Ulaya Magharibi zinawakilishwa na ***Vidole Kumi Vya Nyayo*** (Dan.2:42). Falme hizo ni ***Uingereza***, ***Ufaransa***, ***Ujerumani***, ***Uswisi (Switzerland)***, ***Ureno***, ***Hispania***, ***Italia***, ***Waheruli (Heruli)****, ***Wavandali (Vandals)****, na ***Waostrogothi (Ostrogoths)****. Falme tatu za mwisho huwezi kuziona katika ramani ya siku hizi. Habari zake zitatolewa katika somo la Danieli 7. Mataifa hayo 10 yalikuwa makoloni ya Warumi. Rumi ilipoanguka mwaka 476 yakawa yamejikomboa na kuwa huru. Baadaye yalipoipokea dini ya Katoliki kwa nguvu yakajikuta yametawaliwa na Papa aliyejiita Mfalme wa wafalme kuanzia mwaka 538 B.K.

VII. UFALME WA MILELE WA KRISTO (MAREJEO YAKE HADI MILELE)
Ufalme huo unawakilishwa na ***Jiwe lililochongwa bila kazi ya mikono*** (Dan.2:34,35,44,45). Jiwe hilo ni Kristo (Luka 20:17,18; Mt. 21:42,44; Mdo. 4:10-12). Huyo ndiye ***Mfalme wa Amani*** anayekuja upesi sana (Isa. 9:6; Ufu.22:12). Atakapokuja atazivunjilia mbali falme zote za dunia (Ufu.11:15; 19:11-21). Soma zaidi kuhusu somo la miaka 1000 itakayoanza atakapokuja Kristo mara ya pili, vitabu vya Kiswahili kama ***Majibu kwa Mashaka Yako***. Baada ya kupita miaka hiyo 1000 waovu watafufuliwa na kuangamizwa katika moto wa milele pamoja na Shetani na malaika zake na kuwa majivu, ndipo dunia hii iliyoharibiwa vibaya wakati wa kuja Kwake mara ya pili [Yer. 4:23-27; Ufu. 6:14-17] itakapofanywa kuwa mpya pamoja na mbingu yake (Ufunuo Sura ya 20; Mal. 4:1-3; Eze. 28:14-19; Ufu. 21:1; Zaburi Sura ya 37).

Ombi letu la dhati lingekuwa ni hili: "Ee Yesu, ***nikumbuke*** utakapoingia katika ufalme Wako" (Luka 23:42). Ahadi ile ile itatolewa kwetu kuanzia leo tunapomwomba ombi hilo kama kweli tumedhamiria kuishi kwa ajili yake hapa duniani, "Utakuwa pamoja Nami peponi" (Luka 23:43). Ndugu yangu, kwa nini leo hii uipoteze nafasi hii ya thamani? Kata shauri sasa kumfanya Yesu awe Bwana na Mwokozi wako. Itumie vizuri nafasi ya leo kama yule jambazi pale msalabani. Acha kucheza na dhambi. Leo ndiyo siku ya wokovu wako (2 Kor. 6:2).

## ASOMAYE NA AFAHAMU - 6

## **VIJANA WATATU WASHINDA MTIHANI WA AMRI YA PILI** (SOMA DANIELI 3 YOTE)

Tangu mbinguni Shetani amekuwa akiipiga vita Sheria ya Mungu (Amri Kumi). Anamkasirikia vibaya sana kila mtu anayezishika Amri zote Kumi za Mungu na Imani ya Yesu (Ufu.12:17; 14:12;
Kut. 20:3-17). Mtu akishika Amri tisa katika hizo kumi ni sawa na mtu ambaye hashiki hata moja, kwani zote zi pamoja, mfano ni amri kumi ni kama kioo ambacho kina sehemu kumi, kikivunjika sehemu moja basi ni chote kimevunjika, ; Shetani hana shida na mtu kama huyo, maana yuko upande wake; hawezi kumpiga vita hata kidogo (Yak.2:10-12). Amri Kumi ndizo zinazoonyesha dhambi, kwa maana "***Dhambi ni uvunjaji wa Sheria [Amri Kumi]***" (1 Yohana 3:4, AJKK; Rum. 7:7). Inachukua uvunjaji wa amri moja tu kuwa mwenye dhambi. Kwa hiyo, Mkristo ye yote, haidhuru awe nani au awe na cheo gani, anayeidharau Sheria ya Mungu iliyotolewa mlimani Sinai (Amri Kumi) yuko katika hatari kubwa ya kupoteza uzima wa milele (1 Yoh. 2:3-6; 5:1-5; Zab. 119:155). Yesu aliye kielelezo chetu na ambaye ni Mungu alishika Amri Kumi za Baba Yake; sembuse wewe (Yoh. 15:10). Usikubali mtu ye yote akudanganye,maana "watu wabaya na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu, wakidanganyana kudanganyika" (2 Tim.3:13). Hao waepuke. Angalia usijidanganye mwenyewe (Gal. 6:7,8), wala usimruhusu kipofu akuongoze, kipofu mwenzake, mtatumbukia wote wawili shimoni (Mt. 15:14). Uzima wa milele una thamani kubwa kiasi kwamba mtu hawezi kukubali kuupoteza vivi hivi (Mt. 22:29).

Hapa tunawakuta vijana watatu wa Kiebrania kasoro Danieli hayupo safari hii. Katika Danieli 1 tuliona jinsi vijana wale wanne walivyoshinda mtihani ule wa chakula. Kula chakula au kunywa kinywaji kinachodhuru mwili kwa makusudi mazima ni kuvunja Amri ya Sita inayosema, Usiue (Kut. 20:13). Hivyo walishinda mtihani wa Amri ya Sita. Sasa wamekabiliwa na mtihani mgumu kabisa wa Amri ya Pili inayosema, "Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. ***Usivisujudie wala kuvitumikia***..." (Kutoka 20:4-6). Mfalme Nebukadreza baada ya kuelezwa maana ya ndoto yake aliyoota ya sanamu kubwa katika Danieli 2 kuhusu Falme zile Kuu Nne ukiwamo na ufalme wake akafanya shingo ngumu kupinganana Mungu. Akatengeneza sanamu kubwa ya dhahabu tupu [dhahabu iliwakilisha ufalme wa Babeli] akimaanisha kwamba ufalme wa Babeli utadumu

milele. Akataka sanamu hiyo iliyowekwa katika uwanda wa Dura isujudiwe na wote waliokuwapo pale (Dan.3:1-7). Wote wakaisujudia kasoro wale vijana watatu Waebrania ----- Shadraka, Meshaki, na Abednego. Ni ujasiri ulioje katika halaiki ile walimokuwamo viongozi wakuu wa serikali ya Babeli! Watu wa Mungu wanatakiwa kuwa na ujasiri kama huo kutetea kweli ya Mungu hata kama mbingu zinadondoka (Rum. 8:35- 39; Ebr. 11:32-40; Dan. 11:33). Mfalme alijaribu kuwasihi wafanye hivyo mara watakaposikia tena filimbi na ngoma zikipigwa. Akawatishia kuwa atawatupa katika tanuru ya moto iliyokuwa kali mara saba kuliko kawaida. Lakini wao kwa upole wakasema, “Mfalme, Ee Nebukadreza, hamna haja kujibu katika neno hili. Kama ni hivyo, Mungu wetu tunayemtumikia aweza kutuokoa na tanuru ile iwakayo moto; Naye atatuokoa na mkono wako, Ee mfalme. Bali kama si hivyo,ujue, Ee mfalme, ya kuwa ***sisi hatukubali kuitumikia miungu yako, wala kuisujudia hiyo sanamu ya dhahabu uliyoisimamisha***” (Dan. 3:16-18). Ndipo mfalme akakasirika sana na kuamuru wafungwe na kutupwa na wanajeshi mashujaa ndani ya tanuru ile ya moto. Wale waliowatupa walikufa kwa ukali wa moto ule. Hatimaye wakafanikiwa kuwatupa katikati ya ile tanuru iliyowaka moto. Je! kulitokea nini? Asomaye Na Afahamu - 7

Loo! mfalme akashangaa,hatukutupa watu watatu, mbona wako wanne, na mmoja anakuwa kama mwana wa miungu [Yesu alikuwa pale kuwaokoa]. Ameahidi kuwa atakuwa pamoja na watu Wake mpaka mwisho wa dahari (Mt. 28:20). Hata wakipita motoni au katika maji mengi atakuwa pale tayari kuwaokoa (Isaya 43:1,2). Alitimiza ahadi Yake kwao katika tukio lile la kutisha. Wakawa wanatembea ndani ya moto bila kuungua. Walipotolewa nje ya tanuru ile “wakawaona watu hao, ya kuwa ule moto ulikuwa hauna nguvu juu ya miili yao, wala nywele za vichwa vyao hazikuteketea, wala nguo zao hazikubadilika, wala harufu ya moto haikuwapata hata kidogo” (Dan. 3:27). Bwana asifiwe!!! Ana uweza wa kuokoa kabisa! Mungu anasema, “kwa maana wao ***wanaoniheshimu nitawaheshimu***, na wao wanaonidharau watahesabiwa kuwa si kitu” (1 Sam. 2:30). Ndugu yangu, je! utasimama imara kutetea Amri Kumi za Mungu? Mfalme akatambua kuwa “hakuna Mungu mwingine awezaye kuokoa namna hii. Kisha akawakuza [akawapandisha cheo] Shadraka, na Meshaki, na Abednego, katika wilaya ya Babeli” (Dan. 3:29,30); akawadharau wale wote walioisujudu sanamu ile na kutoa amri kuwa wakisema neno lolote juu ya Mungu wa vijana hao watakatwa vipande vipande na nyumba zao zitafanywa jaa [la takataka]. Hiyo si dharau kubwa? Kuna thawabu katika kusimama imara kutetea Kweli ya Mungu. Yusufu alifungwa gerezani kwa kukataa kuzini, yaani, kuvunja Amri ya Saba (Kut. 20:14). Matokeo yake Mungu alikuwa naye gerezani na hatimaye alitolewa na kuheshimiwa kwa kupewa cheo cha Waziri Mkuu wa Misri (Mwa.39:21-23; 41:37-44). Babeli inawakilisha nguvu za giza [Shetani] zinazopigana na Amri Kumi za Mungu. Hata Babeli Mkuu wa Ufunuo anayo tabia hiyo hiyo. Shetani anaitumia Babeli kutekeleza maangamizi yake juu ya watu wa Mungu wasio na hatia. Kizazi hiki cha mwisho cha Sayansi na Teknolojia kitakabiliwa na Mtihani Mgumu kuliko yote wa Amri ya Nne ihusuyo Sabato (Kut. 20:8-11). Yohana alionyeshwa kwamba kila mtu aliye hai wakati huo atajaribiwa (Ufu. 3:10). Watakaolindwa na Kristo ni wale waliolishika Neno la subira Yake (Ufu.14:12) ---- “Hapa ndipo penye ***subira*** ya watakatifu, ***hao wazishikao Amri [Kumi] za Mungu na***

***Imani ya Yesu***". Je! utasimama chini ya Bendera ya Imanueli iliyoandikwa maneno hayo juu [Ufu. 14:12] au chini ya Bendera ya Chapa ya Mnyama [Ufu. 13:16,17] ---iliyoandikwa siku ya kupumzika ya kizazi kipya kijacho? Hebu kwa neema Yake Mungu na tuazimie kwamba 'hatuwezi kutenda neno lolote kinyume cha ile Kweli, bali kwa ajili ya Kweli" (2 Kor. 13:8). Lakini Kweli ni nini? Neno la Mungu ni Kweli; Sheria ya Mungu (Amri Kumi) ni kweli (Yoh. 17:17; Zab. 119:142). Neno Lake na Sheria Yake hudumu milele (Mt. 25:35; 1 Pet. 1:23; Luka 16:17; Zab. 119:44). Sheria Yake ni "kamilifu"; hivyo huwezi kuongeza wala kupunguza kitu katika Sheria hiyo ya Amri Kumi (Zab. 19:7; Kum. 4:2,10-13).

## ASOMAYE NA AFAHAMU – 8

**KIBURI SUGU CHA MFALME CHASHUSHWA** (SOMA DANIELI 4 YOTE) Amini usiamini, wote tuna kiburi kwa kiwango fulani. Kiburi hicho kinatokana na nafsi, yaani, ***umimi***. Kiini cha dhambi zote ni ule umimi (nafsi). Unaweza kujikweza au unaweza kujidhalilisha isivyopasa. Mambo yote hayo mawilini kiburi. Mwenye kujikweza anasema, "Mimi ni tajiri, mimi ni msomi, mimi... mimi...." Anajiona kuwa yu bora kuliko wengine kwa vile alivyo na kwa vile anavyofanya. Anayejidhalilisha isivyopasa akipongezwa kwa kazi nzuri aliyofanya,anasema, "Si kitu! Sikufanya la maana!...." Lakini moyoni mwake anajipongeza kuwa amefanya vizuri sana. Yule anayesoma mioyo anaandika katika kumbukumbu kuwa hicho ni kiburi. Kiburi kilimwangusha Lusifa mbinguni akapewa jina baya la Shetani (Isa. 14:12-15; Eze. 28:14-17). Wazazi wetu Bustanini Edeni walidanganywa na Shetani kuwa wakila tunda lile lililokatazwa watakuwa kama Mungu. Wakala, wakajiona uchi, wakapoteza utukufu alizoumbiwa, na wazao wao wakawa wamepungukiwa na utukufu huo (Mwa 3:3-7; Rum. 3:23). Mungu anachukia sana kiburi kwa sababu nafsi yetu inataka kumwondoa katika kiti Chake cha enzi mioyoni mwetu na kukikalia yenyewe (Mithali6:16- 19). Tulijifunza katika somo la kwanza (Danieli 1) kwamba miili yetu ni Hekalu la Roho Mtakatifu. Mtu anayeiruhusu nafsi kutawala moyo wake anamfukuza Roho moyoni mwake. Kama kuna vita kali kuliko zote hapa duniani ni ile ya kupiganana nafsi yetu. Nafsi haifi kabisa; inaweza kukandamizwa tu isijitutumue. Kwa hiyo ni muhimu tuwe macho kila wakati ili isije ikajitutumua juu ya Mungu au juu ya watu wengine. Paulo alikuwa na vita iyo hiyo. Anasema, "Ninakufa kila siku" (1 Kor. 15:31). Kwa maneno mengine, "naifisha nafsi yangu kila siku," au "napigana na umimi unaojiinua ndani yangu." Kuweza kuidhibiti nafsi ni kwa njia ya kumruhusu Kristo kukaa moyoni mwetu, "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala ***si mimi [si umimi wangu]*** tena, bali Kristo Yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu" (Gal. 2:20). Nafsi itaondolewa ndani yetu wakati wa parapanda ya mwisho tutakapopewa miili ya utukufu, isiyokufa (1 Kor.15:51-53). Ndiyo maana si vizuri mtu kujisifu kuwa ameokoka, maana anaweza kuangushwa na nafsi wakati wowote na kupoteza wokovu wake (1 Kor. 10:12; Eze. 33:12-16; Mt. 24:13). Kwanza kule kujisifu kwenyewe tu ni dhambi ambayo haina msamaha mpaka mtu huyo atubu na kujishusha kiburi chake (Luka 18:9-14).

Tunaruhusiwakujisifiamsalaba wa Kristo tu uliotuletea ukombozi sisi tusiostahili(Gal.6:14). Sifa zote anastahili kupewa Mungu kwa lolote tufanyalo au kwa mafanikio yetu (Yer.9:23,24). Sasa tunamkuta mfalme Nebukadreza aliyekuwa ameuona uweza mkuu wa Mungu wa kuwaokoa wale vijana watatu katika tanuru ile ya moto, na kukiri kwamba "hakuna Mungu mwingine awezaye kuokoa namna hii" (Dan.3:29), akijitukuza juu ya Mungu huyo kwa njia ya kiburi chake. Mji wa Babeli ulikuwa na utukufu mkubwa sana (Isa. 13:19a). Hakuna ufalme mwingine duniani unaoweza kuwa na utukufu kama ule. Mungu alimpa ndoto ya sanamu iliyowakilisha falme zote zitakazotawala kuanzia wakati wake mpaka Kristo atakapousimamisha ufalme wake (Danieli 2). Kwa kiburi akapinga mpango wa Mungu kwa kusimamisha sanamu ya dhahabu tupu (dhahabu iliwakilisha ufalme wa Babeli) katika uwanda wa Dura na kutaka watu waisujudie. Kwa kiburi alimdharau Mungu wa mbinguni kuwa si kitu; bali kwamba Yeye atadumu milele pamoja na ufalme Wake. Aliishi



na watu wa Mungu ili ajifunze juu ya Mungu wa Israeli; vijana wale wanne walikuwa fundisho kuu kwake. Hakujali yote hayo. Mungu katika upendo wake akamletea ndoto ya pili ili kumwonya aachane na kiburi chake sugu (Dan. 4:4-17). Katika ndoto yake aliona mti mrefu uliokua mpaka mbinguni; wanadamu,wanyama, ndege wote walipata chakula chao katika mti huo. Kisha akamwona mlinzi mtakatifu akiamuru mti ule ukatwe na kibaki kisiki tu kikapate umande wa mbinguni kwa nyakati (miaka) saba. Kwa nini? "Kusudi walio hai wapate kujua ya kuwa Aliye juu anatawala katika ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye, tena humtawaza juu yake aliye mnyonge" (Dan. 4:17). Ni wafalme wangapi wanaofahamu kuwa ni Mungu aliyewaweka katika viti vya enzi wanavyovikalia? (Rum.13:1-7; 1 Tim. 2:1-6). Wajibu wa Serikali zote za dunia ni kusimamia utekelezaji wa Amri Sita za mwisho katika zile Kumi (Kut. 20:12-17). Wanapofanya kazi yao hiyo vizuri na kwa uaminifu na haki mataifa yao yanabarikiwa. Wanapoingilia mambo yanayomhusu Mungu (Amri Nne za kwanza - Kut. 20:3-11) wanavuka mipaka ya madaraka aliyowapa na kustahili adhabu kutoka kwa Mungu. Biblia sio kitabu cha siasa; lakini kuinuka na kuanguka kwa mataifa yote ya dunia kumeelezwa humo. Ni Mungu anayetawala katika falme zote za wanadamu. Mungu anapima nyendo za mataifa yote duniani (Zab. 66:7-8; Zaburi 2; 9:17). Ni jambo la kusikitisha mno kwamba mataifa yote ya dunia, ukiwaondoa watakatifu waliomo, yataangamizwa vibaya siku ile ya mwisho kwa kwenda kinyume na madaraka aliyowapa Mungu (Ufu. 19:11-21).

Danieli alipoitwa kuitafsiri ndoto ile ya mfalme "akashangaa kwa muda, na fikara zake zikamfadhaisha"(Dan. 4:19). Kwa nini alifadhaika? Kwa sababu ndoto ile ilimaanisha kwamba mfalme angefukuzwa mbali na wanadamu na kula majani kama ng'ombe kwa miaka saba. Kwa nini iwe hivyo? Kwa sababu ya kiburi chake sugu. "Nyakati [miaka] saba zitapita juu yako; ***hata utakapojua*** ya kuwa Aliye juu Ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, Naye humpa Yeye amtakaye, awaye yote" (Dan. 4:25). Miezi 12 baadaye, "alikuwa akitembea ndani ya jumba la kifalme katika Babeli. Mfalme akanena, akasema, Mji huu sio Babeli mkubwa nilioujenga ***mimi***, uwe kao langu la kifalme, ***kwa uwezo wa nguvu zangu***,

ili uwe utukufu wa enzi yangu?" (Dan. 4:29,30). Pale pale tangazo likatolewa kutoka mbinguni kuwa ufalme wake umeondoka kwake na atakaa na wanyama akila majani kama ng'ombe kwa miaka saba mpaka atakapojifunza kumtambua Mungu wa mbinguni. Mafunzo ya miaka saba kukishusha kiburi sugu! Fikiria hilo! Mungu na ashukuriwe! Nebukadreza alijifunza kwa njia ya aibu sana (ya kuwa mwehu) kwa miaka saba mizima. Alitoka akiwa kiumbe kipya; akakitubia kiburi chake sugu na kuanzia hapo akaanza kumtukuza hadharani Mungu wa mbinguni (Dan. 4:34,35). Ufalme wake akarudishiwa. Ushuhuda wake mbele za watu ameutoa mwanzo wa Sura hii ya 4. "Mfalme Nebukadreza, kwa watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wanaokaa katika dunia yote; Amani iongezeke kwenu. Mimi nimeona vema ***kutangaza habari za ishara na maajabu, aliyonitendea Mungu aliye juu***. Ishara zake ni kubwa kama nini! na maajabu yake yana uweza kama nini! ufalme wake ni ufalme wa milele; na mamlaka yake ni ya kizazi hata kizazi" (Dan. 4:1-3). Siku moja wale watakaookolewa watakutana na Nebukadreza mbinguni. Atawasimulia vizuri kisa chake. Ni wangapi ambao Mungu anapozungumza nao katika Neno Lake wanakaza shingo zao kwa kiburi na kuyatukuza mawazo yao juu ya Mungu na kufanya kinyume na maagizo Yake? Je, wako tayari kupelekwa porini na kula majani ili wajifunze? Hilo ni zoezi kali mno. Je! Mungu atanivumilia mpaka lini asiukate mti wangu? (Luka 13:6-9). Yatupasa kutubu; la sivyo tutaangamizwa (Luka 13:1-5). Sisi si maarufu kuliko Mungu;wala sisi si bora kuliko wengine.

## ASOMAYE NA AFAHAMU - 10

**USIKU WA MWISHO DUNIANI** (SOMA DANIELI 5 YOTE)
Moyo wa mwanadamu umejaa upumbavu. "Mpumbavu amesema moyoni, Hakuna Mungu; Wametenda uovu wa ufisadi na kuchukiza, Hakuna atendaye mema" (Zab.53:1). Watu wanaopenda kufanya dhambi huamua kumfutiliambali Mungu katika mawazo yao, mafundisho yao, na maisha yao. Biblia inasema huo ni upumbavu. Kwa sababu Yuko Kweli, na watu kama hao watawajibika kwa vitendo vyao viovu. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba hatujifunzi kutokana na yale yaliyowapata watangulizi wetu. Tunataka kujionea wenyewe. Siku moja mfalme Belshaza (mjukuu wa Nebukadreza) alifanya karamu kubwa ya ulevi kwa ajili ya wakuu wake elfu. Hakujua kwamba karamu yake hiyo ilikuwa ya mwisho, na ya kwamba Mungu wa mbinguni alikuwa ameiona hata kabla haijafanywa (Yer. 51:37-40,57-58). Na usiku ule karamu ile ikawa ya aina yake; lakini wahusika hawakuweza kuamka asubuhi yake; walikuwa maiti. Belshaza hakujifunza kutokana na mambo yaliyompata babu yake Nebukadreza (Dan. 5:18-23). Alikuwa anajua yote hayo lakini kwa kiburi kabisa akafanya yaliyomchukiza Mungu wa Mbinguni. Makosa makubwa aliyoyafanya ni haya: Kosa lake la kwanza ni kutumia vyombo vitakatifu kunywea pombe (Dan. 5:1-3). Hakuweka tofauti kati ya vyombo vya kawaida vya kutumia na vyombo vitakatifu vinavyotumika kwa kazi maalum ya Mungu.

Jinsi gani siku hizi waumini hawawafundishi watoto au wenzao kuweka tofauti hiyo? "Makuhani [wachungaji] Wake wameihalifu sheria Yangu [Amri Kumi], wametia unajisi vitu vyangu vitakatifu; hawakuweka tofauti ya vitu vitakatifu na vitu vya kutumiwa sikuzote; wala hawakuwafundisha watu kupambanua vitu vichafu [kama

nguruwe, panya, na kadhalika] na vitu vilivyo safi [kama ng'ombe, mbuzi, kondoo], ***nao wamefumba macho yao***, wasiziangalie ***Sabato Zangu***, Nami nimetiwa unajisi kati yao" (Eze. 22:26). Kutokutambua vitakatifu ni kosa la kufisha. Sabato [Jumamosi] ni takatifu (Mwa.2:2,3; Kut. 20:11; Isa. 58:13,14). Jumapili si takatifu; ni siku ya kazi (Eze. 46:1). Siku ya ibada aliyoiweka Mungu kwa wanadamu wote ni Sabato [Jumamosi] na itakuwa hivyo milele zote (Isa. 66:22,23). Zaka (sehemu ya kumi ya mapato yetu) ni takatifu (Law. 27:30-33). Kuitumia kwa matumizi yetu ya kawaida ni kumwibia Mungu (Mal.3:8-11). Wevi hawataurithi ufalme wa Mungu (1 Kor. 6:9,10). Kumtegemea mchungaji wako badala ya kusoma Biblia mwenyewe ni hatari kubwa! Kosa lake la pili ni kunywa divai [pombe] (Dan. 5:4a). Tulijifunza katika somo la kwanza lililohusu vyakula na vinywaji kwamba pombe inaudhuru sana mwili wetu, na ya kwamba wale wanaouharibu mwili wao kwa pombe au kwa njia nyingine yoyote wataharibiwa (1 Kor. 3:16,17). Pombe ina sumu ya alkoholi/ kileo ambayo inaathiri mishipa ya fahamu, ubongo, moyo, nyama za mwili, na kadhalika. Sio suala tu la kulewa linalohusika, bali ni ile sumu iliyomo. Wengi hata wakinywa pombe nyingi hawalewi; lakini sumu inafanya kazi miilini mwao na kuiharibu. Hivyo wale wasemao kunywa pombe kidogo tu wasingeweza kusema hivyo kuhusu sumu ya panya. Sumu kidogo tu yatosha kuua mtu au kuuathiri mwili (Mithali 23:29-35). Biblia inailinganisha sumu iliyomo katika pombe na sumu ya nyoka aitwaye "fira" (Mithali 23:31,32). Ni sumu mbaya sana. Biblia inasema walevi [wanaolewa na wasiolewa] hawataurithi ufalme wa mbinguni (1 Kor. 6:9,10). Kosa la tatu la Belshaza ni lile la kuisifu miungu badala ya Mungu wa mbinguni (Dan. 5:4b). Neno lasema, "BWANA asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri.

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 11.**

Asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii ya kwamba ***ananifahamu Mimi, na kunijua***, ya kuwa Mimi ni BWANA, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi ***napendezwa na mambo hayo***, asema BWANA" (Yer. 9:6). Si kwamba Belshaza alikuwa hamjui Mungu wa mbinguni alipokuwa anaisifu miungu yake pamoja na wakuu wake, kilikuwa ni kiburi chake sugu kilichomfanya afanye hivyo. Je! wewe unamsifu nani? Wakati sherehe imefikia kilele chake, wamelewa na kuanza kusifu wanawake na miungu yao, kiganja cha mkono kisichotoka damu kikaanza kuandika ukutani. Jasho jembamba likawatoka. Pombe yote ikayeyuka kichwani. Hofu kuu ikawashika, wasijue la kufanya. Wataalam wakaitwa ili wayasome maandiko yale; hawakuweza. Ndipo malkia, nyanya/bibi wa Nebukadreza, akaingiana kuwaambia habari za Danieli jinsi alivyomtafsiria ndoto babu yake. Danieli akaitwa. Akamshutumu Belshaza kwa kiburi chake, licha ya kujua fika yaliyompata babu yake. Akasoma maandiko yale ukutani: "MENE (HESABU), MENE (HESABU), TEKELI (MIZANI), NA PERESI (MGAWANYO). Na tafsiri ya maneno hayo ni hii; MENE, Mungu ameuhesabu ufalme wako na kuukomesha. TEKELI, Umepimwa katika mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka. PERESI, Ufalme wako umegawanyika, nao wamepewa Wamedi na Waajemi" (Dan.5:25-28). Ilikuwa imetabiriwa mapema kwamba milango ya kuingilia mjini itaachwa wazi na maji ya mto yatakaushwa (Isa. 45:1; 44:27). Hivyo ndivyo alivyofanya Koreshi aliyeyaongoza majeshi ya Wamedi na Waajemi usiku ule. Milango ya

mto haikufungwa usiku ule. Wakaingia na kumwua mfalme na viongozi wake waliokuwamo mle. Ulikuwa ni usiku wa mwisho kwao. Mungu anayapima mataifa katika mizani na kukomesha ufalme wao kama apendavyo. Vile vile anampima mtu mmoja mmoja katika mizani ile ya mbinguni (Amri Kumi) na kuandika mbele ya jina lake "umepunguka" au "umetimilika katika Yeye" (Kol. 2:10). Hiyo ndiyo kazi anayofanya Kuhani wetu Mkuu, Yesu Kristo, mbinguni tangu mwaka wa 1844. Karibu sana kesi ya kila mmoja wetu itakatwa kwa milele. Akimaliza kazi yake ya upatanisho au hukumu atatamka maneno haya ya kutisha: "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa" (Ufu.22:11). Hukumu hiyo itakatwa kabla ya kuanguka mapigo yale 7 ya Ufunuo 16. Katika pigo la mwisho atakuja kuwachukua watu wake na kuwaangamiza waovu wote. Mkulima yule tajiri aliyevuna mavuno mengi asijue pa kuyaweka, alifikiri kwamba atakuwa na maisha marefu sana ya raha mbele yake (Luka 12:16-21). Usiku ule akajiambia mwenyewe, "Ee nafsi yangu, una vitu vyema vingi ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi" (Luka 12:19). Maskini yule, alipolala usiku ule hakuamka, aliuawa. Yule mlinzi mtakatifu asiyeonekana aliyeandika ukutani Babeli, akatamka kwa tajiri huyo maneno haya, "Usiku huu wa leo wanataka roho yako! Vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani?" (Luka12:20). Ndugu yangu,leo ndiyo siku ya wokovu (2 Kor. 6:2). Kesho si yako (Yak. 4:13-16).

Amua leo kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wako. Achana na ulevi na dhambi zote. Ukimpokea atakupa uwezo wa kushinda dhambi (1 Kor. 15:57; Yuda 24,25). Usiku wa mwisho duniani kwako na kwangu unaweza kuwa ni usiku huu wa leo. "Basi jiangalieni, mioyo yenu isije ikalemewa na ***ulafi***, na ***ulevi*** na ***masumbufu ya maisha haya***, siku ile ikawajia kama mtego unasavyo; kwa kuwa ndivyo itakavyowajilia watu wote wakaao juu ya uso wa dunia" (Luka 21:34,35). Siku moja ulimwengu wote unaojifurahisha katika anasa mbalimbali za dhambi hautaweza kuiona asubuhi; watakuwa maiti, hawatazikwa, wala kuliliwa (Yer. 25:32-37). Itakuwa karamu ya mwisho Mungu atakayowafanyia ndege (Ufu. 19:17,18).

## ASOMAYE NA AFAHAMU – 12

**AFAULU MTIHANI WA AMRI YA KWANZA** (SOMA DANIELI 6 YOTE) Katika Babeli ya zamani na Babeli Mkuu wa mwisho inadhihirika tabia ile ile ya Shetani ya kuichukia Sheria ya Mungu [Amri Kumi] na kuwalazimisha watu kutenda kinyume na Sheria hiyo. Waliabudu miungu, sanamu, na wafalme. Nimrodi ndiye muasisi wa mji wa Babeli (Mwanzo 10:8-12). Aliabudiwa kama mungu Bel (jua). Bel (Isa. 46:1) ni mungu mkuu wa Wababeli na Waajemi,ni kifupi cha "Baali". Historia inaonyesha kuwa wapagani tangu siku za Babeli waliabudu jua katika siku ile ya Jumapili. Tumeona jinsi vijana wale wanne (Danieli 1) walivyojaribiwa juu ya Amri ya Sita, isemayo, "Usiue" (Kut.20:13). Kula vyakula na kunywa vinywaji vinavyodhuru mwili ni kujiua polepole. Walishinda mtihani ule. Pia tumeona wale vijana watatu (Danieli 3) walivyojaribiwa juu ya Amri ya Pili inayokataza ibada ya sanamu (Kut. 20:4-6); walishinda mtihani ule mgumu japo walitupwa motoni. Mungu alipendezwa kuwaokoa. Pia tuligusia juu ya kujaribiwa kwa Yusufu kule

Misri juu ya Amri ya Saba, inayosema, "Usizini"(Kut. 20:14). Alishinda.

Sasa tunamkuta Danieli (Danieli 6) akijaribiwa juu ya Amri ya Nane, isemayo, "Usiibe" (Kut. 20:15). Alishinda bila shida (Dan. 6:4); alikuwa mwaminifu. Kisha tulidokeza kuwa mtihani mgumu kuliko yote wa siku za mwisho ni juu ya Amri ya Nne, inayohusu Sabato ya Mungu (Kut.20:8-11). Kizazi cha Sayansi na Teknolojia kitaweka siku ya kupumzika nyingine isiyokuwa Sabato. Dunia itagawanyika katika makundi mawili ----- hao wazishikao Amri [Kumi] za Mungu pamoja na Imani ya Yesu, na wale wasiozishika, japo miongoni mwao watakuwamo wanaomwamini Yesu. Kushika Amri Kumi za Mungu ni lazima uzishike zote (Kut. 20:3-17; Yak.2:10-12). "Dhambi ni uvunjaji wa Sheria [Amri Kumi]" (1 Yohana 3:4, AJKK). Tukirudi kule Babeli tunamkuta mfalme Dario aliyempenda sana Danieli, mtu wa Mungu. Kutokana na "roho bora iliyokuwa ndani yake Danieli, alimteua kuwa Waziri Mkuu wa Babeli. Jambo hilo liliwakasirisha sana mawaziri waliokuwa wanawania cheo hicho. Wakatafuta njia ya kumwondoa katika cheo hicho kwa kuchunguza utendaji wake wa kazi na matumizi ya fedha za Dola ile ya Wamedi na Waajemi, "halikuonekana kosa wala hatia ndani yake" (Danieli 6:1-4). Wakakaa kikao cha faragha. Wakatafuta mbinu hii na ile wasiweze kuiona. Hatimaye wakasema, "Hatutapata sababu ya kumshtaki Danieli huyo, tusipoipata katika mambo ya ***Sheria ya Mungu wake [Amri Kumi]***. Naam, wazo hilo likawa zuri na likakubalika kwa wote. Tahadhari ikawa kwamba wasiweke amri yoyote itakayomshtua mfalme maana anampenda Danieli. Wakazipitia amri moja moja wakaona ya kwanza inafaa. Lakini Danieli hawezi kukubali kuabudu mwanadamu, maana amri hii inasema, "Usiwe na miungu mingine ila Mimi" (Kut. 20:3). Wakasema mfalme atagundua tu kuwa tumemlenga Danieli, rafiki yake. Mmoja akatoa wazo kuwa tumhusishe mfalme. Tuseme watu wote waombe kwa mfalme kwa siku thelathini tu; atajisikia vizuri, wala hatajua kuwa tumemlenga Danieli. Wakasema sisi tunajua kwamba Danieli hatakubali na tutakuwa tumemnasa kabisa, cheo cha Waziri Mkuu kitamponyoka; kitakuwa chetu. Sawa? Sawa! Wakamwendea mfalme kwa hila na kumshurutisha kuitia amri hiyo muhuri wake. Soma Danieli l6:5-9. "Basi mfalme Dario akayatia sahihi maandiko yale, na ile marufuku/ katazo" (Dan.6:9). Sheria ya Wamedi na Waajemi haiwezi kubadilika,yaani, haiwezi kubatilishwa ikiisha kutungwa mpaka itekelezwe kama ilivyo.

## ASOMAYE NA AFAHAMU – 13.

"Basi Danieli, alipojua ya kuwa yale maandiko yamekwisha kutiwa sahihi, akaingia nyumbani mwake, (***na madirisha katika chumba chake yalikuwa yamefunguliwa*** kukabili Yerusalemu)" (Danieli6:10). Je! aliomba kimya kimya ili watu wasisikie anaomba kwa nani? "Wakamwona Danieli akiomba dua, na kusihi mbele za Mungu wake" (Dan. 6:11). Alikuwa anaomba kwa sauti kubwa wanasikia dua anayotoa kwa Mungu wake. Ni ujasiri ulioje mbele ya kifo kibaya cha kuliwa na simba! Yesu ameahidi kwamba "kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, Nami nitamkiri mbele za Baba Yangu aliye mbinguni" (Mt.10:32). Danieli alipokuwa anamkiri Kristo waziwazi hata mbele ya kifo mbingu yote ilikuwa inaangalia kila kitu kwa makini sana na kujiandaa kumlinda. Wengi wetu tungekuwa tunaomba kimoyomoyo ili watu wasije wakatusikia na tukahatarisha

maisha yetu. Matokeo yalikuwaje pamoja na juhudi ya mfalme kutaka amri ile isitekelezwe? "Wakamtupa katika tundu la simba" (Dan. 16:16). Wakajipongeza kuwa njama yao juu ya Danieli imefanikiwa kabisa na hawatamwona tena. Mfalme alikuwa na imani na Mungu wa Israeli, ijapokuwa alikuwa na wasiwasi sana juu ya usalama wa maisha ya rafiki yake Danieli, alipoona wamemtupa katika tundu la simba. Akasema Maneno haya, "Mungu wako unayemtumikia daima, Yeye atakuponya" (Dan. 6:16). Mfalme hakulala usiku kucha akifikiria jinsi simba wanavyomrarua vipande vipande rafiki yake; akijilaumu kwa nini hakugundua njama ya mawaziri wale waliomwonea wivu Danieli. Je! simba wale wenye njaa kibao walimla Danieli, Shahidi wa Yesu? Mfalme akaenda kwenye tundu lile la simba, akilia kwa huzuni, "Ee Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, je! Mungu wako, unayemtumikia daima, aweza kukuponya na simba hawa [wenye njaa]?" Danieli akamjibu mfalme, "Mungu wangu amemtuma malaika Wake, Naye ameyafumba makanwa ya simba nao hawakunidhuru" (Dan. 6:21,22). Simba wale wakawa bubu; makucha yao hayakufyatuka, wala hawakuwa na ari yoyote ya kumrukia.

Mfalme akaagiza wamtoe. Amri ya Wamedi na Waajemi isiyobadilika ilikuwa imetekelezwa lakini bila matokeo yaliyokusudiwa. Akatoa amri nyingine isiyobadilika ili itekelezwe mara moja. Akaamuru waliomshtaki kwa kijicho chao watupwe mle mle, "wao, na watoto wao, na wake zao" (Dan. 6:24). Nini kilitokea? "Wale simba wakawashinda wakaivunja mifupa yao vipande vipande, kabla hawajafika chini ya tundu" (Dan. 6:24). Wivu au kijicho kina mshahara wake! Wengi wanatafuta njia ya kuwang'oa wenzao kwenye vyeo vyao kwa kupeleka mashtaka ya uongo au kutega mitego ya hila ambayo huwa vigumu sana kujinasua. Mungu anaouna uovu wote huo. Wahenga walisema, "Mchimba shimo hutumbukia mwenyewe." Biblia inasema, "Mwenye kuchimba shimo atatumbukia ndani yake" (Mhu. 10:8). Siku zile za Esta Hamani akamwonea wivu au kijicho Mordekai.
Kwa siri akachongamti mrefu sana wenye ncha kali wa kumtundikia Mordekai, mtu wa Mungu aliyekuwa hana hatia yo yote kama Danieli.
Matokeo? Alitundikwa mwenyewe kwenye mti ule ule aliouchonga kwa mikono yake (Esta 7:9,10).

## ASOMAYE NA AFAHAMU – 14.

Mfalme Dario alimpenda Mungu wa Danieli. Mungu Naye akampenda mfalme huyo. Akamtuma Gabrieli kumthibitisha katika ufalme wake (Dan. 11:1). Wafalme wengi wangeiga mfano wa mfalme huyu katika kuwasaidia na kuwatetea watu wa Mungu wanaowekewa mitego ya hila ili kuwaangusha. Mungu atawabariki wafalme kama hao. Danieli akashinda mtihani ule mgumu wa kuitetea Amri ya Kwanza. Mfalme akawaandikia watu wa mataifa yote watetemeke mbele za Mungu wa Danieli. Akasema, "Yeye huponya na kuokoa, hutenda ishara na maajabu mbinguni na duniani, ndiye aliyemponya Danieli na nguvu za simba" (Dan. 6:27). Mungu anasema, "kwa maana wao ***wanaoniheshimu nitawaheshimu***, na wao wanaonidharau watahesabiwa kuwa si kitu (1Sam. 2:30). Danieli akafanikiwa chini ya wafalme wawili (Dan.2:28). Vijana wa leo wangeiga kielelezo cha Danieli.

## ASOMAYE NA AFAHAMU – 15.

## FALME ZITAKAZOWAATHIRI WATU WA MUNGU(SEHEMU YA KWANZA)

(SOMA DANIELI 7 YOTE)

Katika Danieli 7 tunazikuta Falme zile zile tulizozikuta katika Danieli 2, ila maelezo ya ziada yametolewa katika sura hii. Tutaigawa sehemu mbili ili iwe rahisi kufuatilia. Sehemu ya Kwanza itatoa picha ya falme zote kuanzia Babeli hadi atakapokuja Bwana Yesu kuusimamisha ufalme wake wa milele. Sehemu ya Pili itahusika na Ufalme wa Pembe Ndogo ambao utawaathiri sana watu wa Mungu katika siku za kufungia historia ya ulimwengu huu. Watu wa Mungu ni Israeli ya Kimwili (Wayahudi) na Israeli ya Kiroho (Wakristo wa Mataifa yote). Soma Warumi 2:28,29na Wagalatia3:26-29,na kurudia somo la Danieli 9 juu ya Taifa Takatifu la Mungu la siku hizi. Kitabu cha ***Danieli na Siku Zetu*** kitatoa maelezo ya kinagaubaga juu ya somo hili. Katika Danieli 2 tuliziangalia falme hizo kwa Mtazamo wa Kisiasa. Tuliangalia tu utukufu wa falme hizo uliopungua kulingana na madini ----- dhahabu, fedha, shaba, chuma, na udongo. Babeli ulikuwa na utukufu kuliko zote (Isa. 13:19). Katika Danieli 7 tunaziangalia falme hizo kwa mtazamo wa Kidini Kisiasa. Tunaona jinsi falme hizo zilivyowaathiri watu wa Mungu (Israeli ya Kimwili na Israeli ya Kiroho). Mungu anatishia kuchukua hatua ya kuziangamiza falme zote zinazotesa na kuwaua watu Wake (Yer. 25:15-38; 46:28); watu wa Mungu ni sawa na mboni ya jicho lake (Zek. 2:8). Kuwapiga vita watu wa Mungu ni sawa na kupigana na Mungu Mwenyewe. Kilele cha Pambano hili ni Vita ya Har-Magedoni ambayo ni vita kati ya Mungu na falme za dunia zinazotaka kuwaua watu Wake, na kwa kufanya hivyo zinapigana na Mungu Mwenyewe (Ufu. 16:13-16).

Tutaona jinsi mataifa hayo moja baada ya jingine falme zao zilivyokomeshwa kabisa. Ufalme wa Warumi wa Kipagani na Ufalme wa Rumi ya Kipapa utapatilizwa katika nyakati za Agano Jipya kwa njia ya zile Baragumu Saba za Ufunuo 8 hadi 11. Ni jambo la kusikitisha mno kwamba falme zote za dunia tamati yake ni kuangamizwa vibaya kwa sababu tu ya kumsaidia huyo "Pembe Ndogo" aitwaye kwa jina lingine "Mnyama" (Ufu. 19:11-21). Ni jukumu letu kuwaombea sana Wafalme, Marais, mawaziri na viongozi wote wakuu wa ngazi zote katika serikali zote duniani ili wasije wakapatwa na mkasa huo aliouandaa Ibilisi (1 Tim. 2:1-6). Maneno ya kawaida tunayotumia mitaani yana maana tofauti katika taaluma mbalimbali. Kwa mfano "kijiko" ni chombo tunachotumia kulia chakula; lakini kwa Mhandisi wa Majengo na Barabara "kijiko" ni aina fulani ya katapila linalochota udongo na kuuweka wanakotaka. Kwa mtu mwenye akili ni muhimu kuuliza, "Una maana gani kusema hivyo?" Ufafanuzi utakapotole waharara yake itapoa. Hivi sasa watu wanaposikia neno hili "Mnyama" hasira zao zinapanda juu kiasi cha kumpa mikong'oto anayelitamka, hata kumpeleka mahakamani. Lakini neno hilo limetumika katika taaluma ya unabii, maana ya "Mnyama" ni "Mfalme"au "Ufalme" (Dan.7:17). Nani atampa mikong'oto mtu anayesema "Mfalme"? Atakuwa na upungufu kiakili.Ya nini kufoka, ndugu yangu? Uliza kwanza, utapata maana yake. Kwa hiyo, huyo Pembe Ndogo ni Mfalme au ni Ufalme. Tutatumia

Sehemu ya Pili kumfafanua ili kila mtu amjue. Kwa maana asipojulikana na watu wote duniani, Yesu Kristo haji; tutaendelea kusota duniani na kuteseka kwa magonjwa sugu, umaskini, dhuluma kwa muda usiojulikana (2 The. 2:1-4). Paulo amerahisisha sana kwa wale wasioujua unabii kumtambua mfalme huyo katika fungu la 4.

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 16.**

Hebu sasa na tuziangalie falme hizo kwa jumla. Wanyama wote waliotajwa ni wakatili. Hii inamaanisha kwamba falme hizo zilifanya ukatili mkubwa. Tutapitia kwa kifupi tu:-

**1. SIMBA ----- UFALME WA BABELI (*606-538 au 605-539 K.K.)**
Ufalme wa Babeli unawakilishwa na Simba (Dan. 7:4; Yer. 4:5-7; Hab. 1:6-8). Katika Danieli 2 umewakilishwa kwa ***Kichwa cha Dhahabu*** (Dan. 2:37,38). Kuhusu ukatili wake soma 2 Nya. 36:17-20; Yer. 21:7. "Mabawa mawili" aliyokuwa nayo simba ni kasi au wepesi wa kushinda vitani (Hab. 1:6-10). *Vitabu vya historia huonyesha miaka tofauti.

**2. DUBU ----- UFALME WA WAMEDI NA WAAJEMI (*538 au 539-331 K.K.)**
Ufalme wa Wamedi na Waajemi unawakilishwana Dubu, mnyama mkali sana (Dan. 7:5). Katika Danieli 2 umewakilishwa na ***Kifua na Mikono ya Fedha*** (Dan. 2:39a; 5:25- 31). "Mbavu 3" ni majimbo matatu yaliyotekwa kikatili sana na ufalme huu, nayo ni Babeli, Misri, na Lydia (sio Libya). Kuhusu ukatili wake soma Isa. 13:17-22; Yer. 51:28- 44.

**3. CHUI ----- UFALME WA WAYUNANI (331-168 K.K.)**
Ufalme wa Wayunani unawakilishwa na Chui, mnyama mwenye machachari sana (Dan. 7:6). Katika Danieli 2 umewakilishwa na ***Tumbo na Viuno vya Shaba*** (Dan. 2:39b; 8:20,21). "Mabawa manne" humaanisha kasi zaidi katika kushinda vitani. "Vichwa vinne" huwakilishawatawalaau wafalme (Ufu.17:9,10) wanne waliotawala baada ya kufa Iskanda Mkuu (Alexanderthe Great). Hao ni majeneraliwake - Cassander, Lysimachus, Seleucus, na Ptolemy. Katika Danieli 8 Iskanda Mkuu ni "pembe mashuhuri kati ya macho ya beberu" (Dan. 8:5,21), majenerali hao wanne ni "pembe nne" za beberu (Dan. 8:8,22). Ukatili wa ufalme huu soma Dan. 8:6,7.

**4. MNYAMA WA KUTISHA ----- UFALME WA WARUMI (168 K.K. - 476 B.K.)**
Ufalme wa Warumi unawakilishwa na mnyama wa kutisha asiye na jina, mwenye pembe 10 (Dan. 7:7). Ulitawala makoloni 10 ya Ulaya Magharibi. Katika Danieli 2 umewakilishwana***MiguuyaChuma***(Dan.2:40).UkatiliwakesomaDan.7:7,23;2:40. Ni ufalme unaovunja-vunja. Hawakutajwa kwa jina ila historia inakiri kuwa utawala uliouangushaUyunani ni Rumi mwaka 168 K.K. Yesu alipozaliwaulikuwa bado unatawala (Luka 2:1-7; Yoh. 11:48).

**5. PEMBE KUMI ----- FALME 10 ZA ULAYA MAGHARIBI (476 B.K. - KUJA YESU)**

Falme hizo zinawakilishwa na Pembe 10 (Dan. 7:8). "Pembe" ni "Wafalme" au "Falme" (Dan. 7:24). Falme 10 zilijikomboa toka ukoloni wa Kirumi ulipoangushwa mwaka 476 B.K. na mataifa ya kipagani ya Ulaya Kaskazini. Falme 10 ni Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Uswisi (Switzerland), Ureno, Hispania, Italia, Heruli, Wavandali (Vandals), na Waostrogothi (Ostrogoths). Katika Danieli 2 zimewakilishwa na ***Vidole 10 vya Nyayo*** (Dan. 2:41,42). Kuhusu ukatili wao soma historia. Zilimsaidia,tena zitamsaidia papa kuua watakatifu (Ufu.17:12-14).

**6. PEMBE NDOGO ----- UFALME WA PAPA AU UPAPA (538-1798 B.K.)**

Ufalme wa Papa hapa unawakilishwa na Pembe Ndogo (Dan. 7:8,20,24). Ufalme huu una majina mengi katika unabii ----- Chukizo la Uharibifu, Mnyama, na kadhalika. Asomaye Na Afahamu – 18 Umewakilishwa na ***Nyayo za Miguu*** (2:33,42). Ukatili wake usio na kifani ulidhihirika katika Zama za Giza (Dark Ages) ulipowaua zaidi ya milioni 50 ya watu wa Mungu uliowaita "Wazushi" (Heretics). Soma Dan. 7:21,25. Tunajuaje kama huo ni Upapa? Soma Sehemu ya Pili ya Danieli 7.

**7. MMOJA ALIYE MFANO WA MWANADAMU -- UFALME WA KRISTO (AJAPO)**

Ufalme wa milele wa Kristo umewakilishwana Mmojaaliye Mfano wa Mwanadamu (Dan. 7:13,14;Mt. 24:29-31).

Katika Danieli2 uliwakilishwana ***Jiwe*** (Dan. 2:34,35,44,45).

Ufalme huu hauna ukatili; raia zake watakuwa na amani milele (Ufu. 7:13-17; 21:l-7). Lakini kabla ya ufalme huo kuja, Hukumu inaendelea mbinguni tangu 1844 kuamua hatima ya falme hizo zinazotesa watu wa Mungu pamoja na adhabu ya waovu wote; ndipo atakuja (Ufu.22:11,12).

## ASOMAYE NA AFAHAMU - 18

## FALME ZITAKAZOWAATHIRI WATU WA MUNGU (SEHEMU YA PILI) (SOMA DANIELI 7:7-14,18,20-28)

Katika Sehemu hii ya Pili tuna kazi moja tu ya kufanya; kuthibitisha kwamba "Pembe Ndogo" inawakilisha Ufalme wa Papa au Upapa. Wanaokamata wachawi wana vigezo vyao vinavyothibitisha kuwa huyo kweli ni mchawi. Mungu Naye ameweka vigezo vyake ili kumtambulisha"Pembe Ndogo" na kuondoa mashaka yoyote waliyo nayo watu kuhusu suala hilo. Tutatumia mafungu ya Biblia huku na huku (Isa. 28:10) pamoja na Ushahidi wa Historia. Kwa nini tusumbuke kuutambua ufalme huo? Kwa sababu ufalme huo utasababisha wanadamu wote duniani watakaoambatana nao kuangamizwa pamoja nao (Ufu. 19:11-21). Kama nilivyosema huko nyuma, ufalme huu una majina mengi katika kitabu cha Danieli na kile cha Ufunuo. Tutajaribu kujenga daraja la kuunganisha Danieli 7 na Ufunuo 13 kwa kuangalia vigezo vichache tu miongoni mwa vingi. Hukumu iliyotajwa katika Danieli 7 imeamua kumwondolea ufalme na kumwangamiza, lakini baada ya kupewa utawala wake wa Awamu ya Mwisho (Dan. 7:26; Ufu. 19:1-3; 18:4-8; 16:1,2,10,19-21; 17:1-11). Kwa maelezo zaidi soma vitabu vya ***Danieli na Siku***

***Zetu*** na ***Ufunuo*** pamoja na ***Pambano Kuu*** au ***Vita Kuu***.

KIGEZO 1: PEMBE NDOGO ILIKUJA BAADA YA FALME 10 KUJITAWALA (Dan.7:8)

Falme 10 za Ulaya Magharibi zilizotajwa katika Sehemu ya Kwanza ya somo hili zilijitawala mwaka 476 B.K. mara tu baada ya Ufalme wa Warumi kuangushwa. Baada ya kuanguka ufalme huo Askofu wa Rumi, ambaye baadaye aliitwa Askofu wa Maaskofu au Papa, alitawala katika mji wa Roma tu mpaka mwaka 538 B.K. alipoitawala Ulaya Magharibi. Historia inaunga mkono.

KIGEZO 2: PEMBE NDOGO ILIZING'OA PEMBE TATU KABLA YA KUTAWALA
Falme tatu zilizong'olewa kwa amri ya Papa (Dan. 7:8,20,24) ni hizi - Waheruli waling'olewa mwaka 493 B.K.; Wavandali (Vandals) waling'olewa mwaka 534 B.K.; Waostrogothi (Ostrogoths) waling'olewa mapema mwaka 538 B.K. Mataifa hayo matatu yalikuwa yanampinga Papa. Yale mengine 7 kufikia mwaka 508 B.K. yalikubali kuwa wakatoliki kwa kulazimishwa na mfalme wa Ufaransa, Clovis, mwana mpendwa wa Papa. Historia inathibitisha.

KIGEZO 3: PEMBE NDOGO ILIKUWA TOFAUTI NA PEMBE ZILE KUMI (Dan. 7:24). Pembe 10 ni falme za kisiasa za Ulaya Magharibi. Pembe Ndogo ni Ufalme wa Papa wa Kidini-Kisiasa. Historia inaunga mkono. Kanisa la Kikristo ulimwenguni halina utawala wa kisiasa (Yoh. 18:33-38). Kwa hiyo, Ufalme wa Papa umepata mamlaka yake kutoka kwingine, si kwa Mungu (Ufu. 13:1,2; 12:9). Hii ndiyo maana wanaouunga mkono wataangamizwa pamoja nao. Serikali zote za kisiasa za dunia zimepewa mamlaka yao na Mungu (Rum. 13:1-7; 1 Tim. 2:1-6). Kwa ajili hiyo zinawaadhibu wahalifu na kuwasifu raia wema. Ufalme wa Papa unawaua watu wema (watakatifu) na kuwaacha hai wahalifu (Dan. 7:21).

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 19**

KIGEZO 4: PEMBE NDOGO ILITAWALA KWA MIAKA 1260 (Dan. 7:25). Wakati mmoja ni sawa na mwakammoja. Kwa hiyo wakati 1 + 2 + 1/2 = Nyakati 3 1/2 = Miaka 3 1/2.
Mwaka 1 una miezi 12. Kwa hiyo, miaka 3 1/2 = Miezi 3 1/2 x 12 = Miezi 42. Mwezi wa Biblia una siku 30 (Dan. 6:7; Mwa. 7:24).
Kwa hiyo miezi 42 = siku 42 x 30 = siku 1260. Siku 1 ya unabii = mwaka 1 wa kawaida. Hivyo siku 1260 ni miaka ya kawaida 1260. Angalia maajabu! Mnyama yule wa Ufunuo 13:1-10,18 alipewakufanya kazi yake kwa miezi ile ile 42 (Ufu. 13:5). Ajabu zaidi ni kwamba Joka lile Kubwa Jekundu la Ufunuo 12 linawakilisha Rumi ya Kipagani iliyotaka kumwua Kristo kupitia kwa Herode (Ufu.12:2-5; Mt. 2:16) na tena linaiwakilisha Rumi ya Kipapa (Ufu. 12:6,14) ambapo tunaona mwanamke (kanisa la Mungu la kweli) akikimbilia nyikani kwa siku 1260 au miaka 1260. Kigezo hiki kinajenga daraja ya kuitambua Pembe Ndogo ya Danieli 7 kuwa ni Mnyama yule kama Chui wa Ufunuo 13. Tabia zinalandana sana. Upapa ulitawala kihistoria kuanzia 538 hadi 1798 B.K., miaka 1260 kamili.

KIGEZO 5: PEMBE NDOGO ILIWAUA WATAKATIFU (Dan. 7:21,25). Zaidi ya watatifu milioni 50 waliuawa katika kipindi cha utawala wa papa cha miaka 1260 kwa kosa la kufuata mafundisho ya Biblia. Aliwaita "wazushi" (heretics); Biblia inawaita "watakatifu". Ni kweli upapa ulikuwa umelewa kwa damu ya watakatifu (Ufu. 17:6). Ni jambo la kushangaza mno kwa kanisa kuua kanisa! Linganisha na Ufu. 13:7. Ni ufalme ule ule mmoja.

KIGEZO 6: PEMBE NDOGO ILIAZIMU KUBADILI MAJIRA NA SHERIA (Dan. 7:25).
Sheria ni Amri Kumi za Mungu (Kut. 20:3-17). Upapa uliazimu kuifuta kabisaAmri ya Pili inayokataza ibada ya sanamu. Angalia Katekisimu za Kanisa Katoliki pamoja na Misale utashangaa. Amri ya Nne inayohusu Sabato akaibadili na kuweka Jumapili badala yake. Kwa hiyo ibada ya Jumapili iliwekwa na Papa kinyume cha Amri ya Nne. Katika kitabu cha Ufunuo Jumapili inaitwa "chapa" au "alama" ya Mnyama, yaani, Alama ya Mfalme Papa (Ufu. 13:l6,17). Katika gazeti la ***The Catholic Record***, London, Ontario, la Septemba 1, 1923 maneno haya yamenukuliwa: "Jumapili ni alama yetu ya mamlaka.... Kanisa li juu ya Biblia, na uhamishaji huo wa utunzaji wa Sabato [Jumamosi] ni ushahidi wa ukweli huo." Sasa zikawa zimebaki Amri 9, sio 10. Akaigawa Amri ya 10 katika amri mbili kufidia ya pili iliyofutwa kabisa.

KIGEZO 7: PEMBE NDOGO INANENA MANENO MAKUU YA MAKUFURU (Dan.7:8,20)
Hapa tutaangaliamakufuru mawili tu. Kufuru la kwanza ni madai ya kuwa yeye ni Mungu (Yoh. 10:30-33). Kwa vipi? Nanukuu: "Papa ana cheo kikubwa mno, tena ametukuzwa mno kiasi kwamba yeye si mwanadamu tu, bali kama ilivyo ni Mungu, tena ndiye aliye Badala ya Mungu." -----Lucius Ferraris, ***Prompta Bibliotheca Canonica***, Gombo la VI, uk. 438,442, chini ya makala "Papa". Cheo cha Mungu alichojinyakulia ni "Baba Mtakatifu" (Yoh. 17:11). Kufuru la pili ni kudai kuwa anao uwezo wa kusamehe dhambi jukumu ambalo ni la Mungu peke yake (Luka 5:20,21). Mungu peke yake Ndiye anayeabudiwa (Mt. 4:10); lakini papa anataka aabudiwe (2 The. 2:3,4; Ufu. 13:4,7,8,12). Linganisha na Ufu. 13:1,5,6. Ni mamlaka moja ile ile. Mungu hataki watu wake wawe gizani kuhusu ufalme huu, japo kwa sasa ulimwengu unauinua juu sana. Hatimaye utakapotawala kama alivyoruhusu Mungu itakuwa kwa maangamizi ya ulimwengu mzima na dunia itafikia mwisho wake (Ufu. 17:8-11; 6:14-17; 19:11-21). Watakatifu watakwenda mbinguni kutawala pamoja na Yesu kwa miaka 1000 (l Thes. 4:16,17(18); Ufu. 20:4). Dunia hii itakuwa imeharibika vibaya katika

**ASOMAYE NA AFAHAMU - 20**

kipindi chote cha miaka 1000 (Yer. 4:23-27). Baada ya kwisha miaka 1000 watakatifu watarudi hapa pamoja na Mji Yerusalemu Mpya (Ufu. 21:10). Ndipo waovu watakapofufuliwa na kujaribu kuuteka Mji Yerusalemu Mpya au Kambi ya Watakatifu. Moto utawala (Ufu. 20:7-10,15). Hiyo ndiyo Jehanum au Ziwa la Moto au Mauti ya Pili (Ufu. 20:14). Jehanum haiwaki sasa. Itawaka baada ya miaka ile 1000 kwisha. Watakaoingia humo watateketezwa na kuwa majivu pamoja na

Shetani na malaika zake(Mal. 4:1-3; Eze. 28:14-19). Hawatafufuliwa tena milele! Ndipo watakatifu watakapoirithi nchi mpya (Ufu. 21:1; Mt. 5:5; 2 Pet. 3:10-13; Zab. 37 yote).

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 21.**

**PEMBE NDOGO YA DANIELI 8** (SOMA DANIELI 8 YOTE) Pembe Ndogo ya Danieli 7 inawakilishaUfalme wa Papa. Lakini Pembe Ndogo ya Danieli 8 inaziwakilisha falme mbili ----- Rumi ya Kipagani na Rumi ya Kipapa. Ni sawa tu na lile Joka Kubwa Jekundu la Ufunuo 12 lenye vichwa saba na pembe kumi ambalo linaziwakilisha falme zizo hizo mbili. Utazitofautisha kwa vitendo vyake tu. Mungu haoni tofauti yo yote kati ya Rumi ya Kipagani na Rumi ya Kipapa. Yesu aliziita falme zote mbili "Chukizo la Uharibifu," yaani, Mamlaka Zinazowaangamiza watu wa Mungu (Mt. 24:15- 22; Dan. 9:27). Danieli 8 na 9 ni kitu kimoja; Gabrieli alishindwa kuendelea kumweleza Danieli habari za Pembe hiyo Ndogo ambayo itawaua watakatifu kiasi cha kustaajabisha kwa vile alikuwa amezimia (Dan. 8:24,27). Baada ya muda kupita Gabrieli alimjia tena Danieli akamwambia anataka kumpa ufahamu wa njozi ya Danieli 8 ambayo alikatisha kumweleza (Dan. 9:20-22). Lakini kwa urahisi wa kuelewa tutachukua kila sura peke yake. Katika sura ya 8 kuna maono ya aina mbili ----- Kondoo mume mwenye pembe mbili (Dan. 8:3,4) ambaye anawakilisha Ufalme wa Wamedi na Waajemi (Dan. 8:20); kisha akaona Beberu mwenye pembe mashuhuri kati ya macho yake (Dan. 8:5-8) ambaye anauwakilisha Ufalme wa Wayunani (Dan. 8:21). Ile pembe mashuhuri ni mtawala wa kwanza Iksanda Mkuu (Dan. 8:21). Zile pembe nne ni majemadari wake wane waliotawala baada ya kufa kwake Iskanda Mkuu (Dan. 8:22). Cassander alitwaa Jimbo la Magharibi; Lysimachus Jimbo la Kaskazini; Seleucus Jimbo la Mashariki (Siria kwenda mashariki), Ptolemy Jimbo la Kusimi (Misri na visiwa). Falme hizo za Kiyunani zilipigana zenyewe kwa zenyewe; hatimaye Seleucus akachukua eneo lote la mashariki, kaskazini, na magharibi baada ya kuwashinda wenzake. Ni katika pembe (ufalme) ya Seleucus ilimotokea Pembe ile Ndogo ambayo inaiwakilisha Rumi ya Kipagani, na hatimaye Rumi ya Kipapa (Dan. 8:9). Kwa maneno mengine Ufalme wa Warumi ulitokea katika eneo la Seleucus alilotawala. Hiyo ni kweli kijiografia na kihistoria. Sasa tutaangalia mambo machache tu juu ya kazi iliyofanywa na Pembe hiyo Ndogo ya Danieli 8. Mungu kwa mkono wa Musa alikuwa amewaonya Waisraeli kuwa atawaletea taifa ambalo lugha yake hawaijui, litawazingira, watakula watoto wao; hayo yalitokea mwaka wa 70 B.K. majeshi ya Warumi yalipouzingira Yerusalemu na kuuharibu kabisa pamoja na hekalu lake (Kum. 28:49-57; Dan. 9:26,27; Mt. 24:15-20; Luka 21:20-24). Ukatili wa falme hizo zinazowakilishwa na "mfalme mwenye uso mkali", yaani, katili, umedokezwa (Dan. 8:23,24).

Wayahudi walijua Kiyunani lakini sio Kilatini. Agano jipya liliandikwa kwa Kiyunani, lugha ya Dola ya Wayunani. Falme zote mbili, Rumi ya Kipagani na Rumi ya Kipapa zilitumia hila katika kutawala kwao (Dan. 8:25). Soma Historia ya Kale. Mpaka hapo ni mambo ya jumla. Sasa na tuangalie vitendo vya falme hizo kwa uchache tu:-

RUMI YA KIPAGANI: Pembe Ndogo ilikua sana kuelekea nchi ya uzuri, yaani, Palestina (Dan. 8:9). Palestina ilichukuliwa na kuwa sehemu ya Rumi ya Kipagani mwaka 63 K.K. "Jeshi la mbinguni" ni watu wa Mungu, "nyota" ni viongozi wa dini (Dan. 8:10: Ufu. 1:20). "Kuangusha chini na kukanyaga" ni kuangamiza au kuua. Ufalme huu ulitimiza hayo mwaka 70 B.K. ulipouangamiza Mji wa Yerusalemu, kisha katika karne ya pili uliua wakristo wengi chini ya Kaisari Diocletian wa Rumi. Hata kabla yake wakati wa Nero mauaji ya Wakristoyalifanyika. Historia inaweka idadi ya waliouawa na Rumi ya Kipagani takriban milioni 3. "Patakatifu pakaangushwa chini" ni kuliharibu hekalu mwaka 70 B.K.
(Dan. 8:11). "Mkuu wa Jeshi" au "Mkuu wa wakuu" ni Kristo mwenyewe (Dan. 12:1;

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 22.**

Ufu. 12:7,8; Yoshua 5:13-15; Ufu. 1:5). Neno "malaika" maana yake "mjumbe". Linaweza kutumika kwa Kristo na kwa viumbe wale wa mbinguni tunaowaita malaika (Ebr. 1:14), au kwa "wachungaji" (Ufu. 2:1,8,12,18; 3:1,7). "Mikaeli" ni jina la Yesu anapokuwa Mkuu wa Majeshi ya Malaika (Amiri Jeshi wa Jeshi la Bwana). Sauti yake ndiyo itakayowafufua wafu (Yoh. 5:25,28,29; 1 The. 4:16), anaitwa Malaika Mkuu. Huyo Pilato, Gavana wa Rumi ya Kipagani, alikabiliana naye ana kwa ana kama ilivyotabiriwa katika Dan. 8:11,25 (Yoh. 18:33-37; 19:1-3,10,11,23,19-22). Alisulibiwa juu ya msalaba wa Kirumi; alipigwa kwa mijeledi ya Kirumi, na kupigiliwa kwa misumari ya Kirumi, na kaburi lake likalindwa na askari wa Kirumi. Unabii huo ulitimia mia kwa mia. RUMI YA KIPAPA: Tutaangalia mambo kadhaa tu, sio yote. Rumi ya Kipapa ili"iangusha Kweli hata chini" (Dan. 8:12). Kweli ni nini? Kweli ni Neno la Mungu, Kweli ni Sheria ya Mungu (Amri Kumi). Soma Yoh. 17:17; Zab. 119:142. Upapa umeikanyaga chini ya miguu yake Sheria ya Amri Kumi kwa kufuta Amri ya pili inayokataza ibada ya sanamu, na kuweka Jumapili badala ya Sabato (Jumamosi) kama siku ya ibada (Dan. 7:25; Ufu. 13:16,17). Jumapili katika unabii inaitwa "Chapa au Alama ya Mnyama", yaani, Alama ya Uwezo wa Mamlaka ya Papa. Sabato inaitwa Muhuri wa Mungu (Ufu. 7:1-4) au "Alama ya Mungu" (Eze. 9:4-11). Martin Luther aligundua makosa (mafundisho potofu) 95. Sasa ni zaidi kuliko hayo. "Kukanyagisha Patakatifu na jeshi"; yeye hajaliangusha jengo la hekalu, ila amegeuza mawazo ya waumini kumwelekea yeye badala ya Kuhani Mkuu, Yesu Kristo, katika Hekalu la Mbinguni kwa kuanzisha ukuhani na misa(Ebr. 4:14-16; 3:1). Kosa lingine ni lile la kutumia cheo cha Mungu cha "Baba Mtakatifu"(Yoh. 17:11). Muda hautoshi kuorodhesha mafundisho potofu yanayoitwa "mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake" (Ufu. 14:8; 17:2). Unafundisha Mapokeo badala ya Biblia (Mt. 15:3-9; Marko 7:5-13). Uliua watakatifu zaidi ya milioni 50 katika kipindi chake cha utawala wa miaka 1260 (538-1798),kiitwacho Zama za Giza (Dan. 8:24,25; Mt. 24:21,22). Waliomo katika mfumo huo wa utawala wanaambiwa watoke (Ufu. 18:4,5). Kuanzia anayekalia kiti cha papa hadi mlei wanatakiwa watoke haraka. Na mamilioni watatoka kwa dhiki kubwa pamoja na kuuawana wale watakaobaki katika mfumo huo (Ufu. 15:2; 20:4).
Katika Danieli 7:9,10hukumu ilifuatia baada ya upapakufanya kazi yake kwa miaka 1260. Hapa pia tunaona hukumu ile ile ikirudiwa kwa maneno haya: "Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa" (Dan. 8:14).

Mpango wote wa wokovu umedhihirishwa katika Hekalu la duniani na lile la Mbinguni (Ebr. 8:1,2; 9:6,7; Law. 16 yote; Law. 23:27-32). Tangu Sinai hadi Yesu alipokata roho msalabani huduma hiyo iliendeshwa na makuhani pamoja na kuhani mkuu na kufikia mwisho wake (Kut. 25:8; Mt. 27:50,51). Yesu alipopaa mwaka 31 B.K. alikwenda moja kwa moja katika huduma ya chumba cha kwanza cha Hekalu la mbinguni (Ebr. 9:11,12) Hukumu au Utakaso au Upatanisho aliyoanza kufanya Kristo kama Kuhani Mkuu. Siku 2300 za Dan. 8:14 ni siku za unabii,ni sawa na miaka 2300 (Eze.4:6). Zilianza kuhesabiwa wakati ule amri ya kuujenga upya Yerusalemu ilipotolewa mwaka 457 K.K. na kukoma 1844 B.K. Kutakaswa kwa Patakatifu ni kazi ya mwaka 1844 katika chumba cha pili cha Hekalu la mbinguni kinachoitwa Patakatifu pa Patakatifu (Ebr. 9:23-26; Ufu. 11:19). Akimaliza atatamka maneno ya kutisha sana yatakayoamua umilele wa kila mmoja wetu, ama kwa uzima wa milele, ama kwa mauti ya milele (Ufu.22:11,12). Ndipo atakuja kuwachukua watu wake na kuwaangamiza waovu. Somo la Patakatifu ni pana sana. Unashauriwa kusoma kitabu cha ***Pambano Kuu***, Sura ya 24 na 25 kwa maelezo ya kutosheleza.

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 23.**

**TAIFA TAKATIFU LA ISRAELI LAKATALIWA**(SOMA DANIELI 9 YOTE) Gabrieli alikuja tena kwa Danieli baada ya kupita muda fulani tangu siku ile aliyozimia ili kumpa maelezo zaidi ya maono yake ya Danieli 8. Unakumbuka Danieli alizimia (Dan. 8:27). Kwa hiyo Gabrieli alishindwa kuendeleana maelezo yake; sasa akaja tena kummalizia maelezo ya maono yale (Dan. 9:20). "Muda wa majuma sabini umeamriwa [umekatwa,umetengwa kutoka katika kipindi kile cha miaka 2300] juu ya watu wako [Wayahudi], na juu ya mji wako mtakatifu [Yerusalemu].... Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake Masihi aliye Mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu. Na baada ya yale majuma sitini na mawili, Masihi atakatiliwa mbali.... Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu..." (Dan. 9:24-27). Kama ilivyo, juma moja lina siku saba, na siku moja ya unabii ni mwaka mmoja wa kawaida. Kwa hiyo, majuma 70 ni siku 70 x 7 = siku 490 au miaka 490. Miaka hiyo inakatwa katika ile 2300 ya Danieli 8:14 na inaanza kuhesabiwa mwaka ule ule wa 457 K.K. ilipotolewa amri iliyofanikiwaya kuujenga upya Yerusalemu. Miaka hiyo 490 kuanzia 457 K.K. inaishia mwaka 34 B.K. Kipindi hicho walipewa Taifa Takatifu la Israeli ya kale ili kutekeleza mambo 6 yaliyotajwa. Walitakiwa kumpokea Masihi kama Mwokozi wao na kupewa haki yake. Lakini alipokuja kwao hawakumpokea kama Taifa (Yohana 1:11). Majuma 7 ni miaka 7 x 7 = miaka 49 kuanzia 457 K.K. hadi 408 K.K. Majuma 62 ni miaka 62 x 7 = miaka 434 kuanzia 408 K.K. hadi 26 1/2 au 27 B.K. Mwaka wa 27 ndio Yesu akajulikana kama Masihi [Mpakwa Mafuta] alipobatizwa na kushukiwa na Roho Mtakatifu (Mt. 3:13-17; Mdo. 10:38). Ni kweli wakati ulikuwa "umetimia" kulingana na unabii wa Danieli 9 uliomhusu Masihi (Mt. 4:17). Majuma 7 + majuma 62 = majuma 69 au miaka 49 + 434 = miaka 483 tangu 457 K.K. ambayo iliishia27 B.K. Kwa hiyo likawa limebaki juma 1 tu au siku 7 au miaka 7 tu kumaliza kipindi kile cha miaka 490 waliyopewa Taifa

la Israeli kumpokea Yesu Miaka 490 - 483 = miaka 7 ambayo ingeishia 34 B.K. (27 + 7 = 34). Katikati ya juma la mwisho, yaani, nusu ya miaka 7 ni miaka 3 ½ "Masihi atakatiliwa mbali" atauawa kikatili. Kwa hiyo 27 + 3 1/2 = 30 1/2 = 31 B.K. Kristo (Masihi) alisulibiwa. Unabii huu ulitimia barabara. Ingawa Taifa la Israeli lilimkataa Masihi katakata kuwa sio Mfalme wao (Yoh. 19:15), walikuwa wamebakiwa na kipindi cha miaka 3 1/2 hadi 34 B.K. cha kuhubiriwa Injili. Siku moja ilipokaribia Pasaka yake ya mwisho kabla hajaingia mjini aliulilia sana mji na kuusikitikia kwa kile kitakachoupata (Mt. 19: 41-44; Mt. 23:37-39). Alitabiri juu ya kuangamizwa kwa mji huo na majeshi ya Warumi mwaka wa 70 B.K. (Dan. 9:26b). Walikuwa wanajivunia hekalu, lakini yeye akawaambia wazi, "Angalieni nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa," yaani, utukufu wake umeondoka mle kuanzia siku ile. Hotuba Yake ndefu ya Mathayo 24 na 25 ilihusu matukio ya siku za mwisho. "Ikawa Yesu alipomaliza Maneno hayo yote, aliwaambia wanafunzi Wake, Mnajua ya kuwa baada ya siku mbili itakuwa Pasaka, na Mwana wa Adamu atasalitiwa asulibiwe" (Mt. 26:1,2). Huo ulikuwa mwaka wa 31 B.K. Kipindi kifupi kabla ya Pasaka hiyo alikuwa amewaambia waziwazi kuwa "Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao ***watapewa Taifa linguine lenye kuzaa matunda yake***" (Mt. 21:43). Ni taifa gani hilo? Kwa nini alisema maneno hayo kwao? (Mt. 21:33-46).

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 24.**

Taifa lingine Takatifu la Israeli ni lipi? Lilipewa lini Ufalme wa Mungu? Bila shaka lilipewa ilipokwisha miaka ile 490 au majuma 70 waliyopewa Taifa la Israeli la zamani. Walikuwa bado wamebakiwa na miaka mitatu na nusu ya kuhubiriwa injili (30 1/2 + 3 1/2 = 34). Muasisi wa Taifa Jipya la Israeli ni Kristo mwenyewe. Aliwaagiza wanafunzi Wake kuhubiri injili kwanza kwa "kondoo waliopotea wa Israeli" na kuwakataza wasiwaendee Mataifa (Mt. 10:6). Hatimaye aliwaambia, "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika ***Yerusalemu***, na katika ***Uyahudi wote***, na ***Samaria***, na hata ***mwisho wa nchi [dunia]***" (Mdo. 1:8). Mwaka 34 B.K. Stefano alipigwa mawe, na mwaka uo huo injili ikaenda kwa Mataifa. Mwaka uo huo Paulo akawatangazia Wayahudi waliomkataa Masihi, akasema, "Ilikuwa ***lazima*** Neno la Mungu ***linenwe kwenu kwanza [umuhimu wa kwanza mpewe ninyi]***; lakini kwa kuwa mnalisukumia mbali, na kujiona nafsi zenu kuwa hamkustahili uzima wa milele, ***angalieni, twawageukia Mataifa***" (Mdo. 13:46). Taifa la Israeli likawa limekataliwa. Tangu 34 B.K. si taifa takatifu tena; wala halijatengewa kipindi kingine maalum cha kuhubiriwa injili kama upendeleo kwao baada ya kanisa kunyakuliwa (1The.4:16,17[18]). Hapatakuwa na mwanadamu hai duniani kanisa litakaponyakuliwa(Yer. 4:23-26). Waliuchezea muda wao waliotengewa na Mungu. Watahubiriwa injili pamoja na mataifa yote katika kipindi kimoja tu kuanzia 34 B.K. mpaka Kuhani Mkuu, Yesu Kristo, atakapofunga kazi yake ya Maombezi katika Hekalu la mbinguni (Ufu. 14:6-12; 15:8; 22:11). Kitakachofuata ni mapigo 7 ya mwisho (Ufu. 16 yote).

Masharti yale yale aliyolipa Taifa Takatifu la Israeli la zamani ndiyo yale yale aliyolipa Taifa Takatifu la Israeli ya Kiroho au Wakristo (Kut. 19:5,6; 1 Petro 2:9,10; Ebr. 8:10). Utii kwa Amri Kumi ndio msingi wa Agano la Kale na Agano Jipya. Hii ndiyo maana

“watakatifu”wa siku za mwisho kama wale wa zamani watakuwa wanazishika Amri Kumi za Mungu pamoja na Imani ya Yesu (Ufu. 14:12; 1 Yoh. 2:3-6). Imani ya Yesu inahusu kumpokea kama Mwokozi na kufuata mafundisho Yake yote (Mt. 28:19,20; Mk. 16:15,16; Yoh. 3:16; 14:21-26). Wakristo wa mataifa mbalimbali wanaitwa “Wayahudi” au “Waisraeli” wa Kiroho (Rum. 2:28,29; 9:6-8; Gal. 3:26-29). Kifo cha Yesu msalabani kilifutilia mbali tofauti iliyokuwapo kati ya Wayahudi na Mataifa; wote sasa wako sawa na wana haki sawa kwa njia ya kumwamini Kristo (Efe. 2:11-22). Tungepiga kelele na kusema, “Bwana asifiwe!!!”. Hakuna tofauti tena. Chini ya Msalaba ule wa Kalvari wanadamu wote ni sawa. Hakuna haja ya kuwatengea kipindi maalum cha kuwahubiri injili Wayahudi. Wanapaswa kuhubiriwa injili sasa; siku ya wokovu kwa kila mwanadamu ni ***sasa***, sio baada ya kanisa kunyakuliwa (2 Kor. 6:2). Kulinyakua kanisa kutaambatana na kuangamizwa kwa yule Chukizo la Uharibifu na wote wanaomwunga mkono (Dan. 9:27; Ufu. 19:11-21).

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 25.**

**VITA VIKUBWA VINAENDELEA NYUMA YA PAZIA** (SOMA DANIELI 10 YOTE)

Ni jambo la kutisha mno kujulishwa kwamba vita vikubwa vinaendelea nyuma ya pazia; hivi havionekani kwa macho yetu ya kibinadamu, ingawa matokeo yake tunayaona. Danieli alifunuliwa, yaani, alionyeshwa vita vikubwa hivyo visiyoonekana; akaelewa kile ambacho alikuwa hajapata kukielewa siku za nyuma (Dan. 10:1). Yohana pia akiwa Patmo alionyeshwa juu ya vita hivyo vikubwa kuanzia vilipoanza mbinguni na kuhamia hapa duniani hadi vitakapomalizika katika vita ile ya Har-Magedoni (Ufu. 12:7-17; 16:13-16; 17:12-14; 19:11-21). Kumbe kuna nguvu kuu mbili zinapambana! ----- ***Mikaeli*** (Kristo) na malaika zake, na ***Joka*** (Shetani) na malaika zake. Ni Pambano Kuu kweli kweli! Wahenga walisema, “Fahali wawili wakigombana, nyasi zinateketea.” Ndivyo ilivyo. Wanadamu ndio wanaoathirika sana katika Pambano hilo. Paulo anasema kwamba sisi tumekuwa “tamasha kwa dunia [malimwengu yote]; kwa malaika na kwa wanadamu (1Kor. 4:9). Tutakimbilia wapi, maskini! Ajabu ni kwamba Pambano hilo linapiganwa ndani ya vichwa na mioyo yetu, japo matokeo yake tunayaona nje. Tutawezaje kujihami basi? Paulo anasema tuvae silaha zote za Mungu ili tupambane na nguvu za giza, si kwa kutumia mabavu bali kwa kutumia Upanga wa Roho, yaani, Neno la Mungu, na Imani, na Maombi ya dhati (Efe. 6:10-20). Ayubu hakujua kilichokuwa nyuma ya mikasa iliyompata kwa mfululizo; lakini hatimaye alijua. Hatujui kwa nini mambo yanatuendea vibaya ingawa sisi tunaomba sana. Kumbe! nyuma ya mambo yote yanayotutatiza kuna vita vikubwa vinaendelea kati ya nguvu za wema na nguvu za uovu. Mungu angetufumbua macho yetu wengi wetu tungezimia kuona jinsi Shetani na malaika zake wanavyowafanya wanadamu au tungekata tamaa kabisa. Unabii wote wa Danieli 2, 7, 8, 9, 11, 12; kitabu cha Ufunuo chote; Mathayo 24 unalihusu pambano hilo au vita hivyo vikubwa. Mungu ashukuriwe ya kwamba ushindi ni wa hakika kwa watu wa Mungu hata kama watakatwa vichwa au kufanyiwa jeuri yoyote (Ufu. 15:2; 20:4; 12:11; Ebr. 11:35-38; Rum.8:35-39). Je, Shetani anafurahi watu wa Mungu wanapofanikiwa kufanya kazi ya Mungu? Hasha. Anaweka vipingamizi vingi ili kuzuia kazi ya Mungu isifanyike kabisa. Kazi ya Mungu inamnyang’anya raia zake aliodhani ni mateka wake; yeye

hataki kuwachilia kamwe. “Asiyewafungua wafungwa wake waende kwao” (Isa. 14:17b). Hata wale waliomponyoka kwenda mkononi mwa Yesu anajaribu kuwapokonya tena (Yoh. 10:27-30). Kwa hiyo, ni vita vikubwa vinavyoendelea nyuma ya pazia mpaka hapo vitakapozimwa na Mungu mwenyewe katika siku ile ya mwisho. Anaweza kutufunulia au anaweza asitufunulie. Kwetu sasa ni vizuri kuelewa tu kuwa tuko kwenye uwanja wa mapambano, na kwamba “hapa sipo mahali pa raha” yetu na hivyo tusijiziuke au kubweteka na kujistarehesha eti tumefika; uchafu umejaa na maangamizo ni mazito sana” (Mik. 2:10). Tunamkuta Danieli amefunga kwa siku 21 akiomba ili Mungu aifanikishe kazi ya ujenzi wa Yerusalemukama Koreshi alivyowatumaWayahudi kuifanya kazi hiyo (Ezra1:2-5). Kazi ile haikwenda vizuri; kulikuwa na vurugu nyingi kutoka kwa Wasamaria ambao hawakutaka hekalu lile lijengwe (Ezra 4). Mashtaka yakaenda kwa Koreshi ili atoe amri ya kusimamisha kazi ile. Kumbe wakati ule ule alipokuwa anaomba Danieli, mfalme Koreshi alikuwa anashawishiwa mawazoni mwake kuisimamisha kazi ile. Kumbe vita vikubwa vilikuwa vinaendelea kati ya Mikaeli (Kristo) na Shetani juu ya suala hilo. Kristo akimshawishi Koreshi kuunga mkono kazi ile, na Shetani akimshawishi Koreshi kuikataza kabisa kazi ile aliyokuwa ametoa amri. Mapambano ya siku 21 yakaulainisha kidogo moyo wa Koreshi.

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 26.**

Ndipo Mikaeli (Kristo) akaja kwa Danieli (Dan. 10:2-9; Ufu. 1:10-15). Danieli alipotelewa na nguvu kabisa mbele za Kristo, akaanguka chini uso ukielekea chini na usingizi mzito ukamshika. Ndipo Gabrieli akamwinua na kumweka katika hali ya kusujudu na kumjulisha sababu ya maombi yake kuchelewa kujibiwa (Dan. 10:10). Kumbe sala ya Danieli ilikuwa imesikiwa siku ile ile aliyoanza kuomba (Dan. 10:12). Kwa nini jibu lilicheleweshwa basi? “Lakini mkuu wa ufalme wa Uajemi alinipinga siku ishirini na moja; bali, tazama, huyo Mikaeli [Kristo], mmoja wa hao wakuu wa mbele, akaja kunisaidia; nami nikamwacha huko pamoja na Wafalme wa Uajemi [Kristo aliendelea kuwagusa mioyo wafalme wa Uajemi waliomfuata Koreshi]” (Dan. 10:13). Gabrieli alijaribu kumshawishi Koreshi kwa siku 21 bila mafanikio, ndipo akaja Kristo mwenyewe na kuugusa moyo wa Koreshi ili kazi ya ujenzi wa Yerusalemu isikwamishwe. Hata sasa malaika wa Mungu wanakuwamo katika Mabunge ya nchi mbalimbali yanayotunga sheria ili kuhakikisha sheria hizo hazitaiathiri kazi ya Mungu ulimwenguni. Malaika waovu wanajaribu kuwashawishi Wabunge kutunga sheria zitakazoiathiri kazi ya Mungu; lakini Malaika wa nuru wanapinga. Ni vita vikubwa hivyo nyuma ya pazia! Ipo haja kubwa ya kuiombea kazi ya Mungu duniani hasa, kwa wakati kama huu. Kwa nini Kristo alikuja kwa Danieli wakati kama ule? Kulikuwa na ujumbe kwa ajili ya siku hizi za mwisho. Gabrieli akampasha habari Danieli, “Sasa nimekuja kukufahamisha mambo ***yatakayowapata watu wako [Israeli ya Kiroho] katika siku za mwisho***; maana maono haya ni ya siku nyingi bado” (Dan. 10:14). Kutokana na maombi ya bidii ya Danieli alionyeshwa mambo yatakayowapata watu wa Mungu siku za mwisho. Alipewa nuru ya kuyaelewa maneno ya Mungu ya kweli. Gabrieli alikuwa tayari kumfunulia zaidi juu ya Maandiko, akasema, “Lakini nitakuambia yaliyoandikwa katika maandiko ya Kweli” (Dan. 10:21). Neno la Mungu ni Kweli; hili linatutakasa tukifanya lisemavyo (Yoh. 17:17; 7:17; 1 Petro 1:22-25; Yak.

2:22). Shetani siku hizi anawashawishi Wakristo wasisomeNeno la Mungu ati kwa sababu wanaongozwa na Roho. Lakini kuna Roho Mtakatifu na "roho ya upotevu", nguvu zote mbili zinawaongoza watu(1 Yoh. 4:1,6). Roho wa Kweli kazi yake ni kutufundisha Kweli, yaani, Neno la Mungu mpaka tulielewe vizuri kabisa (Yoh. 16:13-15; 14:21-26). Roho ya upotevu inatukataza kusoma wala kusikia Neno la Mungu. Yohana ametupa ruhusa kumpima Roho aliye ndani yetu, kujua ni wa aina gani, yaani, kama ni Roho wa Mungu kweli au ni roho ya upotevu. Mtu anayesema "Mimi naongozwa na Roho," halafu anasema, "Sina haja ya kusoma, wala kulisikia Neno la Mungu," huyo haongozwi na Roho Mtakatifu, bali ile roho ya upotevu au "roho zidanganyazo," yaani, "roho za mashetani" au "mapepo" (1 Tim. 4:1; Ufu. 16:13,14). Neno la Mungu linatuimarisha sana, hata pepo zivume namna gani hazitatuangusha (Mt. 7:24-27). Jikite juu ya Mwamba, yaani, Neno la Mungu au Kristo (Ufu. 19:13; Yoh.1:1-3). Neno na Kristo ni kitu kimoja tu. Huwezi kumpokea Kristo; na kulikataa Neno Lake. Usirushwe-rushwe na kila upepo wa mafundisho na kumangamanga huku na kule; omba upewe mafungu ya Biblia kwa kila fundisho, nawe utakuwa salama (Efe. 4:11-15). Jitahidi kusoma Biblia; itakuhekimisha hata upate wokovu wa kweli uliojengwa juu ya Neno, sio juu ya hisia na misisimko (2 Tim. 2:15; 2 Tim. 3:15-17).

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 27.**

**MFALME WA KASKAZINI KUHAMIA YERUSALEMU** (SOMA DANIELI 11 YOTE)

Mungu hawasahau wafalme wanaofanya mapenzi Yake na kuwasaidia watu Wake wanapopigwa vita na Shetani akitumia wanadamu kuwashtaki. Wanadamu wanapotaka kuivuruga au kuikomesha kazi ya Mungu, ujue nyuma yake yuko Shetani; anawatumia. Vita vikubwa [Pambano Kuu] vinaendelea nyuma ya pazia. Hatuwezi kuviona kwa macho yetu. Koreshi, Mwajemi, ndiye aliyeyaongoza majeshi yaliyoiangusha Babeli usiku ule wa mwisho kwa Belshaza (Dan. 5:25-31). Alimwachia utawala wa Babeli mjomba wake Dario, Mmedi. Kama bado unakumbuka masomo yaliyopita, Dario alimpenda sana Danieli na kumpa cheo cha Waziri Mkuu. Pia alimpenda sana Mungu wa Danieli. Kwa hiyo malaika Gabrieli alitumwa kumthibitisha katika kiti Chake cha enzi na kumtia nguvu (Dan. 11:1). Alipotawala Babeli alikuwa mzee wa miaka 62; baada ya kufa kwake Koreshi alitawala Babeli (Dan. 10:1). Katika Danieli 11 tunaziangalia falme zile zile kuanzia Ufalme wa Wamedi na Waajemi mpaka hapo Ufalme wa Kristo utakaposimamishwa. "Kusimama" maana yake kutawala. Ufalme wa Babeli ulikuwa umeangushwa tayari na Wamedi na Waajemi. Sura hii imeandikwa kwa lugha ya kawaida inayoeleweka vizuri kwa kila mtu. Kwa hiyo hatutakuwa na haja ya kutoa maelezo ya kutosheleza. Unabii huu unaendelea kutoka Sura ile ya 10; Gabrieli anazidi kumweleza Danieli mambo yatakayowapata watu wa Mungu katika siku za mwisho (Dan. 10:1). Ajabu ni kwamba sehemu kubwa sana ya unabii huu tayari imekwisha timia. Wahusika katika pambano hili wameelezwa wazi kwa kuonyesha vitendo vyao ambavyo vilitimia mia kwa mia. Jukumu letu hapa ni kuwataja kwa majina yao wahusika muhimu wachache kutoka katika historia ambao walitimiza mafungu yaliyoonyeshwa katika mibano mbele ya majina yao. Hebu sasa na tuwapitie mmoja baada ya mwingine. Wahusika wakuu katika Ufalme wa Wamedi

na Waajemi: ***Dario*** (Dan. 11:1); ***Koreshi*** (Dan. 10:1); wafalme watatu wa kwanza waliofuatana (Dan. 11:2) ambao ni ***Kambiases***, mwanawe Koreshi; ***Smerdisi***; na ***Dario Histaspes***. Yule wa nne aliyekuwa tajiri kuliko wote ni ***Ahasuero***, huyo ndiye aliyechokoza vita juu ya ufalme mdogo wa Uyunani ambao baadaye uliuangusha Ufalme wa Wamedi na Waajemi. Wahusika wakuu katika Ufalme wa Wayunani: ***Iskanda Mkuu (Alexander the Great)*** (Dan.11:3,4) ----- alipokufa akingali kijana mbichi wa miaka 32, naye hakuacha uzao (mtoto) wa kumrithi. Kwa hiyo majenerali wake wanne wakagawana ufalme wake katika majimbo manne (Dan. 11:4); majina yao ni haya: ***Cassander***, ***Lysimachus***, ***Seleucus***, na ***Ptolemy***. Katika ukoo wa Seleucus walitawala wafalme wengi zaidi ya 20 kabla ya Ufalme wa Wayunani kuangushwa na Warumi. Mmojawapo ambaye hakuwa mashuhuri kama baba yake ni yule Antioko Epifani (Antiochus Epiphanes IV) ambaye watu wengine wanamdhania kuwa ndiye "Pembe Ndogo" ya Danieli 7 na 8. Pamoja na kwamba aliwatesa Wayahudi kwa miaka 3 na siku 10 na kulinajisi Hekalu lao, hatimizi vigezo vyote vya "Pembe Ndogo". Alikufa vitani mwaka 164 K.K. ambapo "Pembe Ndogo" ya Danieli 8 itaondolewa madarakani na Mungu mwenyewe (Dan. 8:25); wala hakupambana na Kristo ana kwa ana kwa vile alikufa kabla ya kuzaliwaKristo, wala hawezi kuwa tishio kwa ulimwengu katika siku hizi za mwisho kama ilivyo hiyo "Pembe Ndogo" ya Danieli 7 na 8. Majenerali hao wanne wa Kiyunani waliendelea kupigana wao kwa wao hadi mwisho; Seleucus akachukua eneo lote la Mashariki (makao makuu yakiwa Siria), Kaskazini, na Magharibi Ulaya. Ptolemy akaendelea kubaki na eneo la Kusini (Misri).

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 28.**

Kijiografia wafalme hao wawili waliobaki wakaitwa "Mfalme wa Kaskazini" (Seleucus) akikaa Siria, na "Mfalme wa Kusini" (Ptolemy) akikaa Misri. Ukoo wa kila mfalme uliendelea kutawala hadi Warumi walipoingilia kati. Wahusika wakuu katika Falme hizo mbili za Kiyunani ni hawa: ***Ptolemy Philadelphus*** ----- mfalme wa kusini (Dan. 11:6), binti yake ni ***Bernice***, aliyekwenda kuolewa kwa ***Antiochus Theus***, mfalme wa kaskazini aliyekuwa na mke wake wa kwanza ***Laodice*** (Dan. 11:6). Laodice akijaa wivu alimwua kwa sumu Bernice, na mtoto wake mchanga aliyemzaa, pamoja na wajakazi wake, na mumewe. Kaka yake Bernice aliyeitwa ***Ptolemy Eurgetes***, chipukizi la mizizi yake, alikwenda kulipiza kisasi cha kuuawa dada yake kwa mfalme wa kaskazini (Dan. 11:7-13). Hatimaye Warumi wakaingia katika mandhari hiyo ya vita za kulipizana kisasi kwa wafalme hao wa Kiyunani. Wahusika wakuu katika Ufalme wa Warumi: Ufalme wa Warumi unaingia katika fungu la 14 hadi la 16 la Sura hii. ***Cleopatra***, binti wa watu [wa mfalme wa Misri], alipelekwa kwa ***Kaisari Julius (Julius Caesar)*** kama zawadi ya uzinzi ili ampendelee katika ugomvi wa utawala na kaka yake (Dan. 11:17-19); ***Kaisari Augusto***, mpenda ushuru kwa anasa zake (Dan. 11:20; Luka 2:1-6). "Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba watu wote wa ulimwengu watozwe ushuru" (Luka 2:1, Tafsiri ya KJV). Yesu, Mkuu wa Maagano, aliishi na kuuawa chini ya ***Kaisari Tiberio*** (Dan. 11:21,22; Luka 3:1; Yoh. 18:15 Kaisari Tiberio). Warumi waliingia Palestina na kuwaua Wayahudi (Dan. 11:23-29). Kusimamishwa kwa ***Chukizo la Uharibifu*** ni mwanzo wa ***Ufalme wa Papa au Upapa*** (Dan. 11:31-39) katika kipindi kile cha miaka 1260 cha Zama za Giza. Mauaji aliyofanya kwa watakatifu

zaidi ya milioni 50 yameelezwa katika mafungu 32 na 33. ***Matengenezo ya Kanisa (Reformation)*** yaliyoanzishwa mwaka 1517 na Martin Luther na kufuatiwa na Wana-matengenezo wengine yaliwapatia maeneo ya kukimbilia waliokuwa wanateswa na kuuawa na Papa (Dan. 11:34; Ufu. 12:16; Mt. 24:15,21,22). Kwa njia hiyo mateso na mauaji yali"fupizwa" Mt. 24:22). Katika nchi za Kikatoliki yaliendelea hadi 1798. Ufalme wa Kirumi wa Kisiasa ulioangushwa unaendelezwa mpaka leo chini ya Upapa. Mfalme wa Kaskazini wa Siku za Mwisho Kuhamia Yerusalemu: Mfalme huyo ni tofauti na wafalme wale wa Kiyunani walioitwa "Mfalme wa Kaskazini" na "Mfalme wa Kusini" kuanzia fungu la 5 hadi la 17. Ametajwa katika fungu la 40 hadi 45. Mambo yanayomhusu "Mfalme wa Kusini" wa siku za mwisho katika mafungu hayo bado hayajabainishwa. Dhana zipo nyingi. Yesu alisema, "Na sasa nimewaambia kabla halijatokea, kusudi ***litakapotokea*** mpate kuamini" (Yoh. 14:29). Unabii unaposema kusini ni kusini kwa mfalme huyo wa kaskazini; nchi zitakazopinduliwa zimetajwa pamoja na nchi zitakazompatia hazina. Mfalme wa Kaskazini wa siku za mwisho ni Ufalme wa Papa au Upapa utakapotawalakatika awamu yake ya pili na ya mwisho (Dan. 11:45; Ufu. 17:8-11). Ufalme huo unakwenda kuangamizwa vibaya na Mikaeli [Kristo] hapo atakaposimama {atakapotawazwa mbinguni katika sherehe iitwayo Arusi ya Mwana-Kondoo, atakabidhiwa Jiji Yerusalemu Mpya tayari kumkaribisha mkewe (kanisa) atakapomnyakua toka duniani wakatiwa kuja kwake mara ya pili} (Dan.12:1; Ufu. 19:6-9; 21:9,10). Kwa hiyo, Papa atakapohamiaYerusalemu,"naye atawekahema zake za kifalme [makao makuu] kati ya bahari [ya Kati] na Mlima Mtakatifu [Mlima wa Mizeituni] wa uzuri [Palestina]" atakuwa anautimiza unabii huu. Lakini akiwa pale "ataifikilia ajali yake, wala hakuna atakayemsaidia" (Dan. 11:45), "naye aenenda kwenye uharibifu" (Ufu. 17:11). Ni ajali gani atayopata, ni uharibifu [maangamizi] gani atapata? Soma Ufu. 19:11- 21).

**ASOMAYE NA AFAHAMU - 29**

**HIVI MWISHO WA DUNIA UTAKUWAJE? (SOMA DANIELI 12 YOTE)**

Yapo mawazo mengi wanayosema watu kuhusu mwisho wa dunia. Wengine wanasema watakatifu watanyakuliwa kwenda mbinguni na waovu wote wataangamizwa; dunia itabaki tupu. Wengine wanasema kanisa peke yake ndilo litanyakuliwa; watu waliobaki wataendelea kuishi duniani, na injili itahubiriwa kwa Wayahudi; ndipo Mpinga Kristo atakuja na kufanya mambo yake. Wengine wanasema mbinguni watakwenda tu wale 144,000, watu wengine wote waliobaki makao yao ni hapa duniani; na ya kwamba dunia hii haiwezi kuharibiwa. Kwa hiyo wanaangalia majengo mazuri na kusema moyoni "Nitarithi jumba hili". Je! Biblia inatupa picha gani juu ya mwisho wa dunia? Na tunaposema tunaishi siku za mwisho tuna maana gani? Zilianza lini kuhesabiwa? Hebu Danieli atuambie katika Sura hii ya 12. Mwanzo wa siku za mwisho (Dan. 12:5-7): Tunaona kipindi kile kile cha Danieli 7:25 kinatajwa hapa tena na "mtu yule aliyevikwa nguo za kitani" [Kristo] anayeonekana pia katika Ufu. 10:1-7. Soma pia Mt. 17:1,2; Mk. 9:2,3. Anasema hivi, "Itakuwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati; tena watakapokuwa wamekwisha kuvunja nguvu za hao watu watakatifu, ndipo mwisho wa mambo hayo yote yatakapotimizwa" (fungu la 7). Maneno hayo aliyatoa akijibu swali la mmoja aliyemwuliza, "Je! itakuwa muda wa miaka mingapi hata mwisho wa

mambo haya ya ajabu? (fungu la 6). “Mambo ya ajabu” ni mauaji yaliyofanyika Upapa kamatika zile za Giza ulipoua zaidi ya watakatifu milioni 50, ambayo yaliwashangaza hata Yohana (Ufu. 17:6). Kanisa kuua kanisa ni ajabu kuu! Litakwenda mbingu ya nani? Nyakati 3 1/2 ni miaka 3 1/2 au miezi 42 au siku 1260 za unabii ambazo ni miaka 1260 ya Ufalme wa Papa wa Awamu ya Kwanza (538-1798). Kipindi hicho kimetajwa tena na tena katika unabii (Dan. 7:25; Ufu. 12:6,14; 13:5; 11:2,3; Mt. 24:21,22). Katika Dan. 11:33,34 anasema, “... wataanguka kwa upanga, na kwa moto, na kwa kufungwa, na kwa kutekwa nyara, ***siku nyingi*** [538-1798]. Upapa ulitumia upanga, moto, kifungo, kuteka nyara kama unabii unavyosema katika kuwaua watakatifu. Mateso yalikuwa mabaya mno kuliko ya watu wasiomjua Mungu. Ufalme wa Papa ulioitawala dunia (Ulaya Magharibi) ulivunjwa na Wafaransa mapema mwaka 1798. Kuanzia hapo fungu la Dan.12:4 likaanza kutimia. Maarifa ya kidini, kisayansi na kiteknolojia yaliongezeka kasi kwa namna ya ajabu. Zama za Giza hazikuwa na maendeleo yoyote. Wana-sayansi na Wanadini waliofuata

Biblia walikuwa wanauawa. Mwaka 1798 ndio mwanzo wa “Siku za Mwisho”. Mwisho wake utakuwakatika Awamu ya Pili inayokujaya Ufalme wa Papa ----- “tena watakapokuwa wamekwisha kuvunja nguvu za hao watu watakatifu” (Dan. 12:7). Historia inajirudia yenyewe. Mateso na mauaji ya watakatifu yatakuja tena atakapotawala Papa (Ufu. 6:9-11) ----- “wakaambiwa wastarehe bado muda mchache, ***hata itakapotimia hesabu ya wajoli wao na ndugu zao, watakaouawa vile vile kama wao.***” Wengi hawaamini maneno hayo; lakini wanapaswa kungoja mpaka yatakapotimia ndipo watakapoamini (Yoh. 14:29). Kusimamishwa kwa Chukizo la Uharibifu au Mwanzo wa Ufalme wa Papa (Upapa): Rumi ya Kipagani iliangushwa na makabila ya kipagani ya Ulaya Kaskazini mwaka 476 B.K. Tangu siku za Mfalme Konstantino, mwaka 330, Askofu wa Roma au Papa aliachiwa kutawala mji wa Roma. Kwa hiyo Dola ya Magharibi ya Rumi ilipoanguka,Papa aliendelea kutawala mji ule. Alishika hatamu za utawala juu ya Ulaya Magharibi kuanzia mwaka 538 baada ya kuzing’oa falme tatu - Waheruli (493), Wavandali (534), na Waostrogothi (mapema 538).

**ASOMAYE NA AFAHAMU – 30.**

Mataifa yale mengine ya Ulaya yalipokea Ukatoliki kwa upanga wa Mfalme Clovis wa Ufaransa. Kwa hiyo, yakajikuta yako tena chini ya Papa, (538-1798). Clovis alifanikiwa kuyafanya Wakatoliki mwaka 508 (Dan. 12:11,12). Kuanzia mwaka huo wa 508 zinahesabiwa siku au miaka 1290 na 1335. Chukizo la Uharibifu lilisimamishwa [lilitawala] kuanzia 538 - 1798 (yaani, miaka 508 + 1290 = 1798 barabara). Mwaka ule wa 1798 ukawa ndio mwanzo wa siku za mwisho. Hukumu ikawekwa mbinguni kumpimia adhabu yake mwaka 1844, yaani, mwisho wa miaka ile 2300 ya Dan. 8:14 (yaani, miaka 508 + 1335 = 1843-1844). Mwaka ukianza tarehe 2 Januari unamalizika katika mwaka unaofuata. Kuna heri gani kwa watu watakaoufikia mwaka 1844, mwaka ambao Hukumu ilianza mbinguni? Wale walio na hekima “watajitakasa na kujifanya weupe” (Dan. 12:3,9,10); tena watasimama kama Danieli katika “kura” yao, yaani, ***majina yao yatabaki katika Kitabu cha Uzima mbinguni*** pamoja na watakatifu wote waliotangulia

(Dan.12:13). Isitoshe heri nyingine ni ile ya kufufuliwa katika ufufuo maalum (Dan. 12:2; Ufu.14:13) kwa wale wote walioshiriki kuihubiri Injili ya Milele kwa uaminifu (Ufu. 14:6-12). Injili hiyo inayoitwa “Ujumbe wa Malaika Watatu” ilianza kuhubiriwa 1840-1844na bado inahubiriwa. Ufufuo wa watakatifu wote utafuata mara tu baada ya ufufuo huo wa mseto utakaokuwa na wale waliomchoma pamoja na wale waliowatesa sana watu wa Mungu(Ufu. 1:7; 1 The. 4:16,17[18]). Mwisho wa Dunia Utakuwaje? Tumeona jinsi Ufalme wa Papa ulivyotawala katika Awamu ya Kwanza (538-1798) na ya kwamba unakwenda kutawala dunia tena. Hiyo itakuwa ni awamu yake ya pili na ya mwisho. Maangamizi ndiyo yatakayokuwa mwisho wa Ufalme huo. Mfuatano wa matukio ni huu ----- Papa atawala awamu ya pili, mateso na mauaji ya watakatifu yaanza tena kwa kipindi kifupi sana, Kristo, Kuhani wetu Mkuu, anamaliza kazi yake ya Maombezi katika Hekalu la Mbinguni na kuufunga mlango wa kutubu au wa rehema kwa tamko la Ufu. 22:11. Watu wa Mungu wametiwa muhuri wa Mungu katika vipaji vya nyuso zao; na watu wa Mnyama wamepata alama ya mnyama vipajini mwao na katika mikono yao. Wakati wa taabu unaanza (Dan. 12:1) Mikaeli (Kristo) anapotawazwa (anaposimama) katika Jiji la Yerusalemu juu; pepo za vita zilizozuiwa zaachiliwa na vita inatapakaa kila mahali ikileta maafa mengi(Ufu. 7:1-4), vimbunga na maafa mengine yanatokea,ndipo silaha ya Mungu ya kutisha sana kwa wale walioikanyaga Sabato yake itakapotumika (Mapigo 7 ya Ufunuo 16). Wale wote watakaomfuata Papa majina yao yataondolewa katika kitabu cha uzima (Kut. 32:32,33; Ufu. 13:8). Mtihani wa siku za mwisho ni Amri ya Nne [Sabato](Ufu. 3:10; 14:9,10). Mchezo wa kuiweka Jumapili badala ya Sabato [Jumamosi] utakuwa na athari mbaya mno kwa dunia nzima (Isa. 24:1-6,19,20; Ufu. 19:11-21). Ole kwa wafalme wa dunia hii! Ole kwa kila mtu asiyesimama upande wa Yesu Kristo katika Pambano hili Kuu! Karibu sana litafikia mwisho wake. Watoto wa Mungu wamechoka na dunia hii wanataka kwenda kupumzika mbinguni kwa miaka 1000, na Yesu anasema. “

Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo” (Ufu. 22:11). Je! Wewe u tayari kumlaki Bwana? Je! utasimama imara hata kama mbingu zikianguka, na kuiinua juu Bendera ya Imanueli [Kristo] iliyoandikwa “Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao Amri [Kumi] za Mungu, na Imani ya Yesu” (Ufu. 14:12). Hivi karibuni dunia hii itabaki tupu, ndugu yangu. Kuanzia leo chagua kuingia Paradiso pamoja na Kristo (Luka 23:42,43; 2 Kor. 6:2). Huenda usisikie mwito mwingine kama huu. Amua leo!
Leo unaposikia sauti Yake, usifanye moyo wako kuwa mgumu!

## WAKILI WA MUNGU

Sisi sote ni mawakili wa Mungu kila tulichopewa ni dhamana na tutatoa hesabu kwa mambo matano au sita hivi! Muda, talanta, mali, mvuto, mahusiano yetu, afya, na hata haiba zetu. Uwakili bora kupita wote ni kumwakilisha Mungu ipasavyo na kutembea katika nyayo Zake. Ni kuwaambia watu habari njema nasi pia kuziishi habari hizi njema kwa kutoa muda na mali zetu. Hatuwezi kupenda bila kutoa. Angalia marafiki zako na jinsi urafiki wenu ulivyo; mara nyingi una furaha nao na unajisikia vizuri kutoa hata usipoombwa, unacheka mpaka jino la mwisho kwa sauti

ya juu. Je, Yeye Baba wa upendo anayetupenda na kutukirimia yote mema, vipi? Tujifunze kuishi bila uchoyo na ubinafsi, ndiyo tutapata furaha na afya ya kweli. Roho iliyochangamka ni bora kuliko dawa Sulemani alisema. Hatukuja duniani na kitu na tutaondoka bila kitu. Kwamba tunapenda vya bwerere, au tunapenda sana kupewa kuliko kutoa si jambo jema.

Pengine uwakili mkubwa kupita wote ni kusisitiza kwamba uwakili ni zaidi ya yale tuliyoyaorodhesha kwenye paragrafu ya juu, uwakili wa muhimu sana ni siri za MUNGU za wokovu au injili, kuwaambia wengine upendo wa MUNGU, rehema, huruma, msamaha kwa kifupi kuwaelezea watu wajue tabia ya MUNGU na upendo Wake na kwamba anataka aishi nao milele zote! Watu watajua tu mawakili wa kweli wa MUNGU endapo watatuona sisi na watoto wetu tunapenda watu na tunatenda haki na kuwa wanyenyekevu na kupenda rehema.

Mjane wa senti mbili alipongezwa si kwa sababu ya vijisenti viwili alivyotoa, bali kwa ile sifuri aliyobakiza nyumbani! Mara nyingi tunatoa makombo yetu na vile vinavyotuzidi kwa masikini yatima, wajane au wahitaji. Ila watu tunawaowapenda tunawapa vitu ambavyo pengine hawavihitaji na huku 'tumekomba sufuria lote,' . tujihadhari na hili limenihusu mara nyingi pia, naomba hekima kulikwepa. Yesu alijua kuna wanasiasa na mafarisayo ila hakumwambia yule mjane asitoe sadaka yake, bali alimpongeza kwa kuitoa na huku akijua kuna walafi na wevi kanisani mle! Hii inatudhihirishia kwamba ni wajibu wetu kumrudishia Mungu kile kilicho chake.

Kutoa ni kwa ajili ya usalama wetu na watoto wetu ili tusiwe na tamaa au wivu. Amri ya kumi ni ngumu kuliko zote kutekeleza, maana huioni! Ni rahisi kuona viwivuwivu kwa wale walio na vitu kama wewe huna ukijaribu kuwapangia bajeti jinsi ambavyo wanapaswa kutumia pesa zao kusaidia watu, ikifika zamu yako kupewa na Mungu hizo, unababaisha babaisha kwa kuwapa chenji chenji watu wenye mahitaji, ila watoto wako unawapa vitu wasivyohitaji nao wanaenda kujisifu. Watoto pia nao wataiga mifano yetu.

Rockferller tajiri wa Marekani mkubwa wa mafuta ya Petroli, alikuwa bahili na mchoyo wa mali yake, mwenye hasira na huzuni (miserable). Alipofika umri wa miaka hamsini, aliugua sana. Rafiki yake mmoja alimshauri awe anajitoa kihali na mali kwa wahitaji naye atapona na kuishi vizuri, yaani kwa raha na afya. Alijaribu hili, na aliishi miaka tisini, akitoa ni ajabu! Kuna hata kitengo cha Rockfeller (foundation) nacho kinasaidia mashule, scholarship, vilema n.k. Tusifikiri kwamba watu wanatoa kwa vile wanavyo! La hasha! hiyo ni nusu tu ya hadithi nzima. Yesu alitoa kauli ambayo ilinyamazisha milele lile swali la nani ni jirani yangu kwa kutuonyesha yoyote aliye mhitaji, awe ni jamaa, mtu baki, mchina, myahudi, au asiye wa kikundi na kabila letu ni jirani yetu.

Mara nyingi nimekuwa mchoyo na kukumbuka hadithi niliyosoma nilipokuwa darasa la kwanza. Kwamba mama mmoja alikuwa mchoyo sana. Naye alikuwa na watoto wakambo waliomtembelea Alipoishi, Naye alikuwa na mtego wa paa ambao mume wake aliweka; na aliposikia sauti, alijua paa amenaswa. Akaona kwamba wale watoto watafanya asifaidi ile nyama peke yake na mume wake na watoto

wake wa kuzaa. Aliwaaga wale watoto wakambo waende ghafla kama akiwafukuza waende kwao. Alipokuja akaangalie mtego kumbe ni chui, naye akamvamia na akauwawa kwa vile hakuwa na msaada wa watu wengine.

Mara nyingi nimetaka kupata mwenyewe ambapo ningealika wengine tupate pamoja nikakosa kabisa. Nimekutana na wale wanaokataa kugawa vitu vyao, hata iwe mirathi na kubania na mwishowe ikaliwa na tunutu, au kuleta huzuni nyingi. Mtu hapati furaha kwa vile alivyo navyo. Furaha yaja kwa kumjua Mungu, kumtumikia na kuhudumia watu. Furaha ya ajabu nafikiri ni Mungu Mwenyewe anatoa, ukihudumu au kutoa kitu, unajisikia unavamiwa na tabasamu (smile attack) hata kama umevaa kiraka, una furaha kuliko wanaoishi majumba makubwa. Kuhusu majumba makubwa fasheni hii imeingia ya kujenga majumba makubwa ila hatukaribishi mtu. Mwanamke mshumi alipanua nyumba yake ili akaribishe watu. Tunajenga tupate sifa, na mtu anaweza kusaidiwa na mtu mwenye nyumba ya majani kuliko sisi wenye nyumba kubwa. Wengine tulianza mahali pagumu tukitembea bila viatu, tulipoona wale wenye viatu vingi tulifikiri wana roho za ukatili, na kwamba wangetufikiria tu, nao wangepata thawabu. Leo hii hatutoi vitu vya maana kwa mtu, tunanunua nguo ghali mno, na zikituchosha ndiyo tunampa mtu ili aonekane alipewa na sisi.

Vitu vya dunia vyinapungua thamani, leo ***nanunua kitu kipya na kesho huwa najiuliza***. “kwa nini nilipoteza pesa zangu na kitu ***hiki*** kibaya au kibovu, mbona hakivutii”. Wengine wadai wakitoa kusaidia kazi ya Mungu ‘zangu zitaliwa kanisani , hekaluni au msikitini.’ Hivi kama nimempa mtu pesa ya kumpa mzazi wangu, naye akatumia nitaacha sasa kumpa mzazi wangu pesa kwa sababu ya wizi wa niliyemtuma? Kama kuna watu wanakula pesa za kanisani, washitaki wachukuliwe hatua. Usimpunje Mungu wako na kukosa baraka kwa watu wapitao kama moshi. Endapo unafikiri umempa Mungu sana, uwe na amani moyoni Yeye si dhalimu, atakurudishia ile ambayo unafikiri umezidisha! Chenji yako yote itarudi! Ila kumbuka zaka yaani moja ya kumi ya mapato yako ni ya BWANA. Yaani Neno linasema ukichukua hiyo si wizi bali umepora kama jambazi mwenye silaha (rob). Jambazi ni yule anayechukua kitu cha mtu, mwenye kitu akiangalia, na kwa nguvu au silaha. Mrudishie Mungu 10% ya mapato yake, ili ubarikiwe au niseme ili usilaaniwe. Mwizi anaiba kwa kunyemelea wakati mwenye mali haoni, ni kama mdokozi hivi. Muumini asiyetoa zaka, anafanya ujambazi- kwa kifupi. Yaani anampora Mungu kwa nguvu, na Mungu anajua.

Wanasema, “Nionyeshe ratiba yako ya siku na bajeti yako, nitakwambia usongo wako upo wapi.” ‘Show me how you use your time and your money, I will tell you what is your passion.’ Pia hundi ni karatasi inayoonyesha upendo wako kwa Mungu (Your cheque book is a theological document). Theology ni mafundisho yahusuyo kumpenda Mungu na kumjua. Usibanie banie vitu na kuwanyenga watu wasio na uwezo, ukiwapora vitu kwa namna mbali mbali. Tukifa hatutazikwa na vitu ila tunaweza kuvitanguliza leo mbinguni, vitungoje huko kwa kusaidia wenye mahitaji na kutoa sadaka kwa Mungu anayetupenda kupindukia. Swali zingine ni kujiuliza jinsi unavyotumia muda wako mtandaoni, ni nini kinakula muda wako? Mama mmoja wiki iliyotupa alisema anaangalia video za paka wenye maajabu siku

nzima, Je, wewe unapoteza muda wako kuangalia nini? Hii inaonyesha mungu wetu ni nani.

Kila mtu ana talanta ya muda, hakuna asiyekuwa nayo! Ni kweli pengine hatuna mali, ila muda je? Tumia muda wako na karama zako za roho vizuri! Maana karama za Roho tumepewa kubariki wengine.
Soma vitabu vya uwakili kama "The Blessed Life." Tumia muda kuiombea kazi hiyo pia. Utashangaa utakavyopata upendo na furaha. Nilishangaa sana kwamba bilionea wa nchi masikini kama India ana nyumba ghali kupita yeyote duniani, dola bilioni mbili! Wakati ambapo Warren Buffet bilionea wa pili Marekani, alisema kwamba yeye anaishi nyumba ile ile aliyoishi miaka hamsini iliyopita ya vyumba vitatu vya kulala! Anatembea na gari la kawaida na anaishi maisha ya kawaida. Amehojiwa na wengi; historia ya maisha yake waweza kuipata kwenye tovuti. Watu wengi wa nchi zinazoendelea wanaweza wakawa kama yule mtu ambaye hakutegemea atapata na wanafuja na kuonyesha visivyo kawaida. Watu wawili hawawezi kuwa matajiri kamwe ni waumini na waafrika. Nimefundisha somo hili kwenye uwakili nchi kadhaa kwenye mabara manne. Mwafrika na mtu anayempenda Mungu wana majukumu kwa jamaa zao na kusaidia injili, na kama kweli wanafahamu wajibu huu, wao daima watakuwa hawana pesa za kutosha, hata wakiwa mabilionea. Mwafrika ana ndugu na jamaa na marafiki masikini wengi na jumuiya yake ina mahitaji mengi, hata leo ningepata dola bilioni mia moja ningekuwa na mengi ya kufanya kwani tunaishi kijiji kimoja cha dunia. Albert Sweitzer aliyefanya kazi Afrika ya magharibi kama tabibu alisema wewe umewekwa na Mungu duniani, na kumbuka una kaka zako wahitaji. Daktari huyu alisaidia afya za watu nchi hizo kwa miaka mingi, maisha yake yanapaswa kusomwa na kila mmoja wetu. Tajiri Rockfeller alipofariki, mhasibu wake aliulizwa na gazeti "Je, aliacha fedha ngapi?" Alijibu, "Aliacha zote!" –he left it all. Hakuna mahali alipozichukua. Aliziacha hapa duniani.

Hata tukiwa na vitu vingi hatuwezi kuvitumia. Naweza kuvaa viatu jozi moja kwa wakati mmoja, au kulala kwenye nyumba moja kwa wakati mmoja au kuendesha gari moja kwa wakati mmoja. Na hata tukiwa na pesa sana hatuwezi kula Tanzanite au dhahabu. Tutakula wali, maharage, ugali au mboga tu. Tufundishe watoto wetu kuwa wakarimu na kusaidia wale wenye mahitaji kwa hali na mali.
Maisha yetu duniani tukizaliwa tunasema wacha ngoja niende shule nitakuwa na raha na kuridhika, kisha tunasema wacha nipate kibarua au nichume hela nitakuwa na raha, kisha wacha ngoja nioe na kuwa na watoto nitakuwa na raha, kisha wacha nistaafu nitakuwa na raha, kisha wacha nipate wajukuu nitakuwa na raha, kisha wacha watoto wajitegemee basi nitakuwa na raha, mwishowe uzee unaingia na tunasema mimi sina raha na siku hizi mara magonjwa na udhaifu, kisha kuwategemea watu kunaingia. Bibi yangu mzaa mama mwaka wa 1969 alikuja kututembelea tukiwa Arusha, alikuwa na miaka 48, nilimwona ni mzee sana, nikasema bibi wewe ni mzee hivi. Alinijibu 'Grace nilitazama tu upande huu nikigeuka nikajikuta ni mzee!, haikuchukua muda, hata wewe utazeeka na utashangaa miaka imeenda wapi!'. Ni kweli nilikuja Marekani nikisema nitakaa miaka sita mpaka leo nimekaa miaka mingi nje ya nyumbani zaidi ya ndani, na sasa nina umri wa miaka kadhaa kumshinda bibi mwaka 1969, na nashangaa hivi muda umeenda wapi?

Hatukuja na vitu duniani na wala hatutaondoka na kitu. Isipokuwa tunaweza kutuma vitu vyetu mbinguni kabla ya wakati (advance) kwa kufanya matendo mema, ndipo nondo na kutu hawatakula mali zetu hapa duniani. Toa vitu vyako mpaka ikuume, si vile ambavyo ulikuwa unataka kuvitupa. "Nilikuwa na njaa ukanilisha, nilikuwa na kiu, ukanipa chakula, nilikuwa uchi ukanivika, nilikuwa gerezani ukaja kunitembelea," tunaambiwa kwenye Neno kwamba hiyo ni pasipoti ukifanya kwa moyo wako na siyo kulazimishwa. Hebu tuombe hili ili tuwe mawakili wema, na tusije ambiwa, "Ondokeni Kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari ibilisi na malaika zake.". Mimi kwa neema ya Mungu sitaki kwenda motoni, wewe Je? MUNGU atatuhukumu kwa mabaya tunayotenda, na pia yale mazuri ambayo hatutendi (commision and ommision). Najua kuna watu ambao sio wema, utakaokutana nao ambao hao hawataridhika hata uwatendee mema,

Neno la Mungu lasema ufalme wa Mungu ni kama lulu kubwa ambayo mtu alipogundua katika aliuza kila kitu na kwenda kuinunua. Tukiwa wadogo tuliimba wimbo wa sauti ya Yankee Doodle, "Mkulima mwenye shamba alipanda viazi, akachimba chimba akaona almasi. Lo! Lo! Bahati ya mtu mwenye shamba, akatupa jembe upande akaenda zake mjini, kununua gari lake sasa ni tajiri. Lo! Lo! Bahati, Loo; Loo; bahati ya mtu mwenye shamba." Ufalme wa Mungu ni kitu cha thamani, kwako wewe mpenda afya ni vyema uuze vyote na kununua huo. Usikazane kujiwekea hazina duniani sana na kujawa na tamaa ya pesa, maana kwa maumivu watu wengi wamejichoma sana. Watu wengi wamefanya mambo ya ajabu kwa ajili ya pesa, "Shina la maovu yote ni kupenda pesa." Pesa itakubadilisha tabia, jihadhari, watu wengi wakiwa hawana pesa wanajua jinsi ya kuangalia wengine na kuona udhaifu wao wa tamaa ya kupenda pesa; ila wakiwa nayo wanajisahau kwamba na wao wana shida hiyo hiyo. Mara nyingi tuna tamaa ya vitu moyoni ila haionekani kwa vile tu maskini. Masikini ana tamaa pia ila hana fursa ili watu wauone huo uchu wa mali. Kamwe usiache kurudisha zaka (moja ya kumi). Hebu watoto wako wafundishe watoto wako kurudisha zaka na sadaka na kutoa sadaka. Buni miradi na kuwalipa hata kama ni pesa kidogo ili waweze kutoa sadaka kutoka katika akiba yao wenyewe, na si ya mzazi wakifika umri wa miaka nane hivi.

Kuna tabia ya wengi wetu kuwatendea mema wale tunaowapenda na si yeyote yule anayehitaji msaada wetu. Hata watu wabaya wanafanya hivyo kwa ndugu zao na marafiki zao. Utamaduni wa sisi waafrika kumpa mtu tusiyemjua ni mgeni. Kama ni watoto yatima tutatunza wa ndugu zetu, kama ni kumsaidia mtu tutasaidia ndugu zetu. Hiki nawasifu ndugu zetu wazungu sana kwani wanaweza kumpa mtu wasiyemjua hata shirika au taasisi fulani, kama vile watoto yatima, utafiti wa kansa n.k. Sisemi usahau ndugu zako; la, hasha! Kusahau ndugu zako ni kama kuwa kafiri. Ila katika ukarimu wako, ukisaidia watoto wa ndugu zako yatima sita, msaidie na mwingine mmoja usiyemjua mwenye mahitaji.

Nimekutana na mhubiri mmoja na mke wake, aliyeniambia yeye kipato chake ni kidogo na ndiyo maana hatoi zaka. Nilimwuliza anakula nini na kuvaa nini? Je, ana shamba? Basi atoe mazao yake. Wanawake wengi au waume wengi wamewakataza wenzi wao kutoa zaka, **usiingie** dhambi hii. Watu wawili wanaona vitu kwa ubora kuliko wewe peke yako ukiwa ndiyo bosi wa kamati ya mtu mmoja

kuamua pesa zitumiwaje nyumbani mwako. Zaka ni kwa ajili ya manufaa yetu na si ya Mola. Yeye ana kila kitu. Nikimpa senti mbili tatu zangu au nikiacha, Yeye hawi masikini kamwe; ni kama mtoto wako mdogo unayemfundisha asiwe na uchoyo kwa kumwomba kiazi kidogo ulichompa akumegee. Hata hivyo kama unafikiri umempa Mungu zaidi ya unavyopaswa kumpa, Yeye si kama mfanya biashara anayengoja uende bila chenji kamili ili aichukue! Yeye ni mwaminifu, na kama ulimpa kupita inavyotakiwa, atakurudishia tu! Hakuna aliyetoa kwa Mungu akafilisika. Haleluya!

Wakati Musa akiandika Torati na kuongoza wa walikuwa na mafanikio ya kupita mpaka walikuwa wa ikitoa 33%; ambayo ni theluthi ya mapato yao! Kulikuwa hakuna mwenye njaa. Jumuiya ***ilibuni*** vitu vya kufanya ili kila mtu awe na kitu cha kumudu maisha au kupata riziki za kukidhi malazi, makazi na chakula. Mpangilio wa Mungu daima unakufanya uwe na heri na fanaka. Wape watoto wako na watu mitaji ya kujiendeleza na wasimamie ukiwa na ujuzi au umtafute mtu wa kuwaendeleza. Watu wengi wenye uwezo wanalia lia, au wanakuwa matapeli kuwaahidi watu mambo makubwa kisha hawaonekani, bali wanayeyuka tu. Wengine walipokuwa hawana uwezo walifuata watu wenye uwezo daima, walipopata afuteni walisahau watu. Walikumbuka watu walipohitaji mahusiano au kupata wateja wa kusikiliza ukubwa au maendeleo yao yalivyo. Wazungu husema huwezi kumpa Mungu zaidi ya anavyokupa, eti ukampita au ukamovertake, haiwezekani "You can not outgive God". Anza kumtumikia Mungu na kumpenda Mungu kwa usongo na ushujaa mwingi. YEYE atakuwa njozi, utume, usongo na nyenzo (vision, Mission, Passion and provision)

Mvuto wako ni muhimu sana. Watu wanapokupenda na kukutetemekea, usitumie nafasi hiyo bila kuwa na hekima. Au mtu akijitolea kwako ili umfanyie ubaya usikubali. Mchungaji Kulakov wa Urusi alisema alipokuwa anafundisha watoto wa Sekondari, msichana mmoja alimpenda sana na alimwambia Mwalimu nimekupenda sana akiwa peke yake, na alitaka wawe na urafiki au amwoe. Mwalimu Kulakov alimwambia mama yake, naye akasema "Mpendwa kijana wangu, watu ambao wako chini ya mamlaka yako wakikupenda na kutaka kujitoa kwako, usitumie mamlaka yako vibaya, hata huyu msichana angekuwa mtu mzima usikubali urafiki wake, labda uamue kumwoa, usiharibu maisha yake eti kwasababu yeye amekupenda". Nilimjua Dwight Nelson mhubiri kule Michigan. Siku moja nikiwepo alitoa kisa cha safari yake, wiki hiyo. Alisema aliendesha kwenda Kalifonia akitoka Michigan, umbali wa kama kilomita 4000. Gari lake lilikuwa Honda ***kuukuu***. Alisema aliharibikiwa gari, mara saba hivi. Baada hotuba yake, wiki iliyofuata walijitolea kama watu kumi hivi kumnunulia gari jipya! Alikuwa na mvuto (influence). Angeweza kununua gari lake, ila aliwaambia watu wale walete hizo pesa waingize kwenye huduma ya kusaidia wenye mahitaji. Je una yatima wangapi, wajane wangapi, masikini wangapi au wageni wangapi unawaosaidia leo katika maisha yako. Najiuliza mwenyewe pia swali hili! Naomba utafakari maaana ndiyo utu wa binadamu na dini ya Kweli ilipo. Jipime na jichunguze leo. Je una magari yamezagaa zagaa nje ya uwanja wako, na utakapoaga dunia watagombania watu ambao hawakuyatolea jasho? Basi anza kuyagawa mahali penye mahitaji. Tajiri Colgate alimpenda Mungu sana, alitoa zaidi ya 10% kwa watu wenye mahitaji na

kusaidia kazi ya Mungu ili watu wengi waende mbinguni, ila alipokufa alisahau kuandika mirathi. Watoto wake hawakujali watu wala Mungu na wakatumbua zile pesa wakisahau yale baba yao aliyoyasimamia. Leo hii weka mirathi, haimaanishi utakufa haraka ukiweka mirathi. La hasha. Watoto wako uwape vitu vichache tu vya kusaidia wawe na bidii ya kazi na kuendelea kuendesha maisha yao bila ufukara sana. Unapowakuza waonyeshe wewe unajali masikini, wajane, na yatima na kujilinda na mawaa. Katika Israeli ulikuwa mpango wa Mungu kila familia iwe na ardhi ili umasiki usiwepo. Watu wenye ardhi kamwe hawawi masikini wakiwa na bidii ya kulima. Nchi zilizoendelea zilianza kwa kujitosheleza chakula na kutunza kwenye maghala, ndiyo wakaghafilika na kuanza kununua silaha, wasingenunua silaha bila kitu tumboni!

Kutotoa zaka Ni kama ukimtembelea mtu ukiwa umempelekea kapu la vyakula (shopping), na vitu vingine kama zawadi, halafu ukishaondoka anakatalia hata lile kapu. Kiafrika, hata hapaswi kurudisha lile kapu likiwa tupu. Atajitahidi atafute hata kitu kidogo aweke ndani. Utamwonaje huyu mtu? Kwamba hana shukrani hata kidogo. Ndivyo tunavyomtendea Mungu wetu. Baada ya kutukirimia na mengi, tunakatalia hata kapu! Lakini tukitoa tunabarikiwa. Alisema tumjaribu, tuone kama Hatafungua madirisha ya mbinguni na kutumwagia mibaraka. Watu wengine wamebarikiwa kutoa zaidi ya 10%; walipobarikiwa kama mfamasia mmoja kule Uswiss, alitoa 90% kama zaka maana alibarikiwa na mahitaji yake yote. Usijali vitu vidogo vidogo kwa ubahili nawe ukavihesabu.

Kama una vingi, fanya kama ujumbe wa Yohana mbatizaji “Mwenye makoti mawili ampe moja mwingine”. Ukiwa hauongezeki saizi huna haja ya kununuanunua nguo na vitu. Msafiri wa mbinguni pesa zako zilete roho siyo vitu. Hata hivyo Roho Mtakatifu, si roho ‘Mtakavitu’ kama asemavyo rafiki yetu mwinjilisti Mukangara. Rahisisha maisha yako, wanasema vichache ni vingi (more is less). Yaani una vichache kwa kutazama ila moyoni una furaha na mengi yanayoburudisha roho mpaka unajiona tajiri zaidi ya Bill Gates kwa vile Mungu amekupa roho ya kuridhika, na amekupamba, hata ukivaa kitu kisicho cha thamani watu wanauliza umepata hiki wapi jamani? Unanawiri ni ajabu. Nafikiri mbinguni patakuwa pazuri si sana kwasababu ya vitu bali kwaajili ya furaha moyoni, yaani pale kwenye mto maji yakitiririka, unaburudika, na kutabasamu, na wapendwa nao wanafurahi nawe, mnapiga masoga, kisha Malaika wanapita kuja kukaa nanyi, kisha Mungu anazungumza nanyi. Hata usipewe kitu yaani taabu zako zimeisha, una shida gani tena, kisha hakuna kifo, huzuni, vilio, maumivu, wala yote si mabaya. Si mambo ya vitu la! Dhahabu kule itakuwa lami tu ya kila kinjia.

Ukiwa una talanta, una sura nzuri, haiba nzuri, mwandishi mzuri, n.k Tumia haya yote kwa kuongoa roho. Siyo yakuletee kiburi, kwamba “Mimi ndiyo mwenyewe.” Uwe mnyenyekevu. Unajua mnyenyekevu hajitambui? Mtu mmoja aliyekuwa mnyenyekevu sana hata alipewa medali na kijiji chake ya unyenyekevu. Siku iliyofuata alipoivaa, ilitwaliwa, kwa vile alikuwa anajitangaza unyenyekevu!

Panga bajeti yako vizuri ili usiwe na madeni madeni. Hali ya madeni na hasa ya nyumba imenipata; naomba usiku na mchana yanitoke. Ogopa madeni kama vile ukoma. Wiwa upendo tu. Ukiwa na madeni unampunja Mungu sana kwa kulipa madeni, maana waweza kwenda jela. Na hilo wengi twaogopa kuliko kumwibia Bwana; hata kama hutoi sadaka au zaka bora ulipe deni; ni hatari. Hata tunasema

eti Mungu anaelewa kwamba nina madeni, nisipotoa zaka na sadaka.

Jifunze bajeti uishi kutokata na kipato chako. Usinunue usichohitaji au kuishi kwenye madeni. Wanaume wengi wanapokea pesa, na kupanga matumizi wenyewe. Mke ana mahitaji mengi, hasa kama hafanyi kazi. Ila fanya hivi: Jiweke kwenye viatu vyake, kwamba yeye ndiye mwenye mshahara nawe huna senti bali yeye hakushirikishi kabisa, mradi anakupa taarifa kidogo hapa na pale inapobidi! Watoto wa nyumba hii wanagundua wakianza kufanya kazi wanamtumia mama tu na wala si baba. Watoto wengi wanaanza kuchukua mama zao kwenda mjini wakiacha mababa wabahili wenye roho mbaya wakijipulizia moto na kuchemsha ugali wenyewe. Baba hawa walikasirika maana walisaidia watoto kusoma kwa kiasi ila wakiamua tu (at their convenience). Wengine naoishi nao karibu wameleta mama zao ughaibuni, baba akawa anatoa dua lisilompata mwewe, yaani halimpati mke, ila linawapata watoto. Watoto wanapaswa kujali wazazi wao, hata kama wazazi hawakujali. Ni dhambi kumtelekeza baba hivyo au mama. Mama huyu apaswa amtetee mume wake na mzazi mwenzake. Mara zingine wakina mama wanaleta picha kwamba wameteswa sana na wanakuwa si wakweli kusema mema mengi ya mume wanavyopaswa. Tujihadhari sana tutachuma dhambi kwa Mungu. Nakumbuka nilipogombana na mume wangu na kukasirika mtoto wangu wa miaka saba aliniuliza na nikamweleza, akajibu 'mama usijali, akija baba toka kibarua mimi na mdogo wangu tutamchangia tumpige'. Mdogo wake alikuwa na miaka mitatu. Hapo ndiyo nilingamua kwamba hata mimi nilikuwa na makosa makubwa tu kwenye huu ugomvi. Hata mume wangu ndiye alikuwa sawa. Na sasa nataka kuwaingiza watoto wadogo kwenye chuki na ugomvi wa muda mrefu na kisha walaaniwe kwa kumchukia baba yao na kutomsaidia kweli? Niliomba Mungu anihurumie na kunisamehe. Najua amenisamehe.

Zamani nilipokuwa sina madeni nikisikia mtu ana shida nilitoa. Siku hizi nalia lia madeni! Madeni! na wala sitoi. Tusaidiane kuombeana tabia hii tukome na Mungu atupe vipato. "Niende mbele za Bwana na mikono mitupu?" Ulisema wimbo wa watoto. Eti kwasababu nina mkopo wa nyumba au shule? Ni aibu, kama wewe ni maskini, na huna yaeleweka; ila ni aibu na si baraka kwako. Fundisha watoto wako kutoa sadaka na zaka.Wakuone unaitoa kila inapotolewa ibadani Sabato. Punguza mambo ya electroniki wakati mwingine waone unatoa fedha halisi! Watajuaje kweli? Wafundishe jinsi ya kutumia pesa, najaribu hilo kwa watoto wasije wakakumbwa na yaliyonipata. Utasaidiaje watu wanaohitaji kusaidiwa kama unakopa kopa, na ambavyo si vya lazima. Yatima au huduma fulani za kushuhudia watu na kuwaleta kwa Bwana.

Usisahau kutunza jamaa, "Mtu asiyetunza jamaa zake ni mbaya kuliko asiyeamini." Wengine waambiwa wazazi wao 'Korban'. Hii inamaanisha kwamba hawawezi kuwasaidia kwa vile vitu vyao vimewekwa wakfu. Mtu ambaye ana kitu na anashindwa kutunza wazazi wake au ndugu zake ni kama kafiri. Naelewa ndugu wengine hutawaweza, wana tamaa kibao, na wanaona wivu ukifanya kazi ya Mungu. Na mara zingine wanapenda wakutawale maisha yako, Omba Mungu usiwe na roho ya chuki.

Ndugu zako na hata mke/mume wako, watakuendesha usisaidie watu wenye mahitaji. Watatazama kwa wivu unampa nani, nini na kusema wawafanya wawe masikini. Japo sijaona anayemsaidia masikini akawa masikini. Ahadi za Mungu ni

za kweli kabisa. Na wengine wakiona unapatana na mume wako au mnaishi vizuri kwa amani na kumfanyia kazi Bwana; na miji yao wanapiganapigana wanasema "mke wake kamkalia." Tafsiri yake mara zingine ni, mke asipendwe, akipigwa kofi ndiyo mambo sawa! Au, 'wanajidai wazungu.' Hivi wazungu ndiyo walikuwa Edeni kwanza au ndiyo wanaopendana kuliko waumini kweli? Hivi wao ndio wana upendo wa agape kweli? Mbona wanaachana kila kukicha na ***kesi za*** kuuana ni zaidi ya kwetu? Au utasikia "wanajidai tu tutawaona, wataachana tu!" Hivi wewe unaombea maanguko ya wenzako tu? Saa ngapi utapata saa ya kujiombea mambo yako kweli, utakaa na kutishia watu mpaka lini kweli, na sote ni wenye dhambi tunaojitayarisha na siku ya hukumu!
Mtu mmoja alifurahi na kucheka wakati mtoto wa mwenzake anaharibikiwa akisema, "Amejiunga kwenye kundi letu. Amekuwa kama sisi, au watoto wake watakuwa wabaya kuliko wangu!" Na huyo mtu hakukuuliza kuhusu ya watoto wako hata pengine alikuombea. Mtu mmoja alimwona bwana mmoja akimfungulia mke wake mlango wa gari akasema, "Mambo mageni haya; nafikiri ni mke mpya au gari jipya!". Usiwe mtu wa kutaka wenzako washindwe, waombee. Mungu bado ana uwezo, mbona Sauli akawa Paulo bila hata yeye mwenye kuomba?

Tuliishi na rafiki yangu na mke wake Michigan. Walinionyesha barua waliyoandikiwa na kaka yao aliyewasomesha wakiwa sekondari, "Mpendwa tulikusomesha, na tumekuambia utununulie lori na trekta, mpaka leo hujatununulia, umeenda Marekani na sasa umebadilika, tutaomba Mungu akukatekate miguu ndiyo utatukumbuka nasi, na kutuona wa maana!" Rafiki hawa walilia machozi, kwani walikuja kusoma kwa kujitegemea, na walikuwa wakisaidiwa kodi na kufanya vibarua vidogo vidogo vya kubangaiza ili kuponea maisha, mwingine alikuwa akilinda makaburi ya wazungu, mwingine akibadilisha wazee wa kizungu nepi nk (survive). Utakumbana na jamaa wa namna hii, ila hilo lisikupe homa ukaacha kuwasaidia wenye mahitaji ukiwa nacho. Kila siku ukiamka, mkabidhi Bwana mipango yako na umwombe akuongoze.

Tembea na vitabu na visome ukiwa unangoja kitu a basi mahali. Wape watu zawadi ya vitabu vizuri. Sio kutabasamu na kukenua nao meno tu, bila ya kuwapa kitu Chema kama unacho. Mvuto si wewe ukwezwe, bali Mungu aonekane katika maisha yako. Hata ukiwa umejaliwa nyumba nzuri, karibisha watu na uwaambie kwa upendo hukumu inayoijia dunia karibuni. Unajua Maandiko yanasema Mungu ana vitabu vitatu. Kimoja ni cha kurekodi mambo. Vitabu hivi vitaletwa hukumuni siku moja na kila tendo tulilotenda liwe jema au baya litaletwa. Filamu ya maisha yetu itapita pale na kila tulichofanya kitaletwa cha kila mmoja wetu. Na pengine hata vile tusivyovifanya tunavyopaswa kuvifanya! Unayakumbuka yale mambo unayoyafanya ya siri, ambayo hutaki hata mume, mke, mtoto, dada, kaka, bibi, babu, mjomba, mpwa, shangazi, au mtu yoyote ajue? Yote yataletwa. Ila zile dhambi tu ambazo zimeungamwa hazitaletwa. Mungu akitusamehe anafuta yote na mfuto wake mkubwa na kuzika dhambi zetu chini sana kama baharini Pacific kule Mariana Trench ambayo kilindi cha maili saba. Japo dhambi zetu ni nyingi na nyekundu kama damu zinakuwa kama theluji ya mlima Kilimanjaro tukiziungama. Je, leo mpendwa msomaji umeungama dhambi zako na toba ili ufungue ukurasa mpya wa maisha yako?

Mifano mingine ya kuonyesha watoto wako ni kwa kusaidia watu ili wajisaidie; siyo wakutegemee wanasema mfundishe mtu kuvua samaki na si kumpa samaki tu ili akutegemee daima. Wape watoto elimu au ardhi ili wajitegemee, wasaidie yatima na wajane. Kwenye kitabu cha Ron Sead "Rich Christians in the World of Hunger", yaani "waumini matajiri kwenye ulimwengu wa njaa, anaeleza mambo ya ajabu mno! Anasema utafiti umeonyesha kwamba, Mwenyezi Mungu Amekuwa mwaminifu ni ajabu, (nitakufanya kichwa na wala si mkia)! Akasema 80% ya utajiri wote duniani umo mikononi mwa waumini wanaokiri Jina la Mungu na Masihi. Akasema shida ni mabahili ajabu! Mungu ametubariki na matrilioni ila tukitoa msaada kwa maskini tunatoa chenji, chenji tu. Badala ya kupanga program za kuwakomboa watu wasitutegemee. Badala ya kutoa jozi ya ng'ombe, mbuzi au miradi itakayozalisha, tunatoa unga au kitu ambacho watakula kisizae ili kesho watuombe tena! Huu ni ukatili wa aina fulani. Ni vyema mno watu hawa uwape elimu, na mitaji midogo midogo ili wajikwamue. Hebu Wasiwe daima mbele yako wakikufagilia na kukusujudu tu.

Wachina wasema ukitaka kufanya tofauti kwa siku moja kula chakula kwenye hoteli nzuri. Ukitaka kufanya tofauti kwa mwezi mmoja oa/olewa (mfano mbaya). Ukitaka kufanya tofauti kwa mwaka mmoja panda bustani. Na ukitaka kufanya tofauti maishani 'panda mtu;' yaani saidia watu kupata elimu, au peleka watoto shule. Utakuwa umemkwamua mtu.

Mara nyingi tumejikuta tukisema kwamba masikini hawa ni waongo, hawahitaji msaada, na pengine ni wavivu. La! Ajabu tulipokuwa na hali mbaya au maskini, hatukufikiri haya, tulitaka tusaidiwe, na tukashukuru. Sasa tukiwa na hali nzuri tunapepeta mengi kuhusu jinsi ya kusaidia watu na kusema lazima nichunguze mno kama ni wakweli, kwani hawa watu ni waongo. Nimechunguza mara nyingi na nikagundua ni lazima niwe mwangalifu, kwani ni Mungu anayepima waongo na tochi yake. Hajanikabidhi kazi hiyo, au Je, wewe amekukabidhi? Wengine tumesema, nikimpa msaada, aenda kunywea pombe, ni kweli, ila ni lini wewe, utamsaidia mjane, yatima au maskini ukifanya machambuzi haya mengi? Maneno ya "Nilikuwa na njaa, kiu, uchi, jela;" hayakuzungumzia kwamba ufanye utafiti wa kuwaumbua. Mungu atajaji. Hatusemi uwasaidie watu wasiohitaji, ila wengi wetu hatuko tayari kutoa, na tunapata sababu ya kuchelewesha utoaji au kutotoa, kwa kisingizio cha 'utafiti wa mwongo asiyehitaji msaada.'. Mara zingine nimependa kuangalia picha za maafa ya watu, watu kwenye mafuriko, tunaona kwenye runinga au kwa macho "yulee anaenda masikini". Ila hata senti hatutoi, na wala hatuwaombei kama hatuna senti. Hivi ni haki kweli, maafa ya watu yawe burudani ya video machoni na wala yasiniume hata nitoe dola moja ya kusaidia mtu anayepatwa na huzuni vile?

Usiache mtu akuombeombe na kukutegemea. Waumini wengine ni wachungu au bahili sana wakiwa na vitu, ila wanapokuwa hawana wanajua jinsi ya kuwapangia walio navyo kufanya kazi ya Bwana au huduma. Tunavaa nguo na vitu vya fahari, rafiki toka Tanzania alijisifu kwangu eti suti yake ni ya dola 5000! Ila tukisikia watu wenye shida tunatoa chenji chenji ndogo ndogo tu, na tunafikiri tunawapwaga watu, kumbe maskini tunajipwaga vibaya!

Sasa napenda kuzungumza na wale wenye maneno mabaya wakiomba vitu na kuwakashifu watu na kuwacharaza kwa maneno! Kama hali yako ni mbaya na unahitaji msaada, hii haina maana wewe ulaani watu na kuwapa maneno ya matusi

na masimango. Uwe na adabu unapoomba msaada na uheshimu watu, hata akiwa ndugu yako, yeye utamwacha afanye uchaguzi wake wa kukupa, huna haja ya kumnyanyasa.

Nashindana na uchoyo, na kuomba Mungu kila siku niendelee kutoa; maana hatuwezi kumgusa Muumba bila kugusa viumbe vyake. Wengi tu 'shaba iliayo na upatu uvuma'. Hata ukiwa na vitu vingi sana; huwezi kuvaa viatu viwili kwa wakati mmoja, kuendesha magari matatu kwa wakati mmoja au kulala vitanda viwili kwa wakati mmoja. Hata nikikutembelea hauwezi kusema leo hapa ***tutakula*** dhahabu na almasi. La; hasha! Utakula ugali ule ule na mboga ***ile ile***, au vyakula vya kawaida tu, la sivyo matumbo yatadhurika! Toa vitu vyako mpaka vikuume, siyo kutoa chenji chenji hata zikidondoka mfukoni mwako ***huzitupii jicho.*** "Mjane wa senti mbili, alipongezwa kwa vile alivyobaki navyo na siyo alivyotoa"
Angalia kama nyumbani mwako kuna vitu vilivyozagaa zagaa, vitoe. Mimi navyo vimesheheni nyumbani, mitumba ambayo nafikiri siku moja nitatuma mahali! Mama mmoja aligundua ana kaseti na DvD kama 200 hivi ambazo alikuwa ameangalia na wala hazitumii! Aliamua kuziuza na zile pesa atumie kwenye kazi ya Bwana. Usiwe mtu wa kulundika vitu vya bohari, ukifikiria kwamba kesho utapata shida na kuvihitaji, wape wengine na Bwana hatakutindikia kesho. Siyo mzungu tu eti anatoa kwa mtu asiyemjua, la Mwafrika pia, maana anajua uchungu wa umasikini.

Ndugu yangu toka Mara, niliona amejaza nguo tele kwenye makabati yake, hata vyumba vingine. Nguo nyingi za watoto za zamani. Anakaa nazo tu akikumbuka watoto wake walivyokuwa wadogo walivaa hichi au kile kiatu mguu wa mtoto ulikuwa mdogo! Shida hii nilikuwa nayo pia, mpaka rafiki yangu, Grace Zuzo wa Afrika kusini aliponiambia, "Ukiwa na nguo 20 au 30 zatosha kwenda kibaruani, na nguo yoyote ambayo huivai zaidi ya mwaka si yako wape watu wengine.". Mara zingine tumepata kuleta macontainer ya nguo, na vitu kwa wahitaji ila tumepata matapeli au ugumu wa kukomboa bandarini, lakini hii haina maana tuache kusaidia mtu kabisa au kutofanya utafiti wa kufanya mambo bora. Mara nyingi na rafiki yangu Zuzo tumeomba Mungu atusaidie kuishi karibu na mpaka wa Mexico au Sudan ili tuwe tunarusha vitu kule kwa watu maana tunapoishi watu hutupa nguo kwenye takataka, na wengine hutupa chakula bure, hatujakata tamaa kuna siku Mungu atafungua milango, tunatamani maombi yenu.

"Nimegundua kwamba ninapotoa nguo zangu kuwapa watu, si sadaka ya dhati mara zingine. Kwani mara nyingi fasheni ikiisha au zikinichosha nazitoa kwa watu maskini. Ni kweli watu masikini wanapata ila utoaji wangu unakuwa na walakini. Maana nguo ninazonunua ni ghali, ila siko tayari kutoa pesa kusaidia mahitaji ya kazi ya Mungu na nipo tayari kutoa mitumba ikinichosha kwa maskini."

Nimekuwa nikitafakari haya. Nawe pia waweza kuyacheua haya. Kwamba unanunua kitu ili uwe nacho kwanza uonekane uko kwenye fasheni kisha unagawa, yaweza kuwa sawa kama unampa binadamu, ila kama ni Mungu itabidi utathmini tena. Kama unasali nao kanisa moja, au unaishi nao kijijini, unawadhalilisha ikiwa kila mtu akiona wanavaa mtumba wako wanajua ni wewe ndiye umetoa.
Wengine wamekuwa na tabia ya kujenga nyumba kila mji zisizoleta kodi, bali

gharama kuzitunza. Tukiweka vibarua tuje mara moja kwa mwaka watu wa kule masikini watushabikie, tajiri amekuja. Alinichekesha rafiki wa Korogwe aliyesema kwamba nyumba yake haikuwa na watu miaka mingi; hata kenge waliingia na kuishi mle. Mambo ya kununua vitu usivyopima vizuri ni shida, ila kama ni rasilimali ni sawa. Wengine wamejenga majumba makubwa kama mapango na kushindwa hata kufuta vumbi kwenye vyumba vingine. Watoto walishaenda makwao, Mtu anasumbuka kupiga deki na kutoa buibui, badala ya kufanya kazi ya kuhudumia watu. Mambo ya majumba makubwa Afrika yalikuwa hayapo, ila sasa yameingia, wakati wazungu wanataka kuyapunguza, sisi ndiyo tunayakolezea moto. Wazungu wana majira ya wakati wa baridi, kwa hivyo waishi majumbani siku nzima. Sisi tuna hali nzuri ya jua, twaweza kuwa na nyumba ndogo, na kukaa nje na kupata hewa bora na jua! Ndugu zetu wamasai wanaingia kulala majumbani na si kushinda humo, hii ni afya

Siku hizi kuna shida ya mali na muda wa kutunza hivyo tunashauri viongozi wa kiroho wasiwe na watoto zaidi ya sita. Huu si ulimwengu wa kuzaa watoto kumi kama zamani. Rafiki mmoja alisema, "Mpaka mayai yaishe. Mungu ametuumba tuwe na watoto, hivyo nitazaa wale atakaonipa." Mungu ameumba pia mizunguko ya mwili ya siku salama ambazo mwanamke hashiki mimba. Tumia hizo, maana hata kama una uwezo, saa ngapi utajitayarisha na hukumu ya Mungu inayotujia karibuni ukiwa una watoto wadogo kwa muda miaka 30? Ila Ulizia njia za uzazi wa majira zisizoua mimba iliyotungwa. Siku hizi mapambano ya kulea watoto ni mazito, jihadhari usikwazike, maana watoto ni kitu cha maisha yote, hata wakipigana huko na mke au mume, watarudi kwako tena uanze upya na wajukuu kwani upendo wa mzazi ni mwingi.

Ni rahisi kuwa mwema kwa watu tusiowajua, ila maneno yetu yanakatakata watu wa karibu. Lazima tuwe na unyenyekevu mahali pote. Kwenye kitabu chetu cha malezi ya watoto, wazazi wengi, hasa sisi kina mama tuna maneno ya kufisha watoto moyo. Hatuyaamini, ila tunayatamka kwaajili ya hasira tu: "Hutafaa kwa lolote maishani mwako!" Hilo ni kofi kubwa, afadhali umchape mtoto kiboko. Au "Mbwa wewe kama baba yako!" Kweli haya ni maneno ya binadamu aliyeumbwa na mfano wa Mungu kweli? Ukichanganua:- mbwa anazaa mbwa, na kama wewe umeolewa na mbwa ulifanyaje uchaguzi huu? Maneno yetu ni uwakili pia, je, wewe unapenda kutukana-tukana, maneno machafu yanakutoka saa yote kwa watu wa nje na ndani, na mahasira. Acha, haisaidii afya katu. Tafuta sabuni na Chlorite na mswaki uoshe mdomo kila unaponena maneno machafu nawe utayaacha. Tuepuke uhodari wa matusi. Doug Batchelor wa Amazing Facts, alinipa moyo. Alisema aliendelea kutoa lugha za matusi baada ya kumjua Mungu kwa miaka michache. Alikuwa mhubiri wa nguvu akihubiria watu kila mahali. Ila aliendelea kuzidiwa nguvu na matusi. Mwishowe alipiga magoti na kuomba; "Bwana midomo yangu ni michafu, najaribu kutotoa matusi, ila nikikasirika natupa makombora yoyote, nisaidie." Alisema kutoka siku hiyo matusi yote yalimtoka. Ni ombi langu pia Mungu anisaidie matusi yanihame pia. Na ukipata ushindi kwa Neno lolote jema mshukuru Mungu na utoe ushuhuda. Wanasema kushuhudia wema wa Mungu kunamwangusha Ibilisi chini 'wakamshinda Ibilisi kwa ushuhuda wa maneno ya mdomo wao na Kafara ya Masihi".

"Safari ya maili 1000 huanza na hatua moja." Tulitoa nadhiri kwa Mungu kwamba akituwezesha kumaliza shule tutarudisha 25% kwake kama zaka na sadaka na kusaidia wenye mahitaji. Nipolimaliza shule na kupokea dola 2000 kwa mwezi, nilihama nilipokuwa naishi ili kupisha wengine wapya kusaidiwa na wamishonari wema; kisha nikaanza kutoa 25% mpaka 50% kwa zaka, sadaka, na wenye mahitaji. Mungu alibariki na tukashugulika na wachungaji na walei tofauti, kujenga vikanisa 80 hivi, (bush churches) na kupeleka watenda kazi (walei) 350 kwenye kozi mbali mbali. Wachungaji na walei pia walitufanya tuwe na ubia (patner) wao kwa kufanya mikutano ya hadhara ya uinjilisti 65 hivi.

Imekuwa safari ya imani, na tuligundua kwamba mkristo hana mpaka, lolote lile muumini afanyalo jiunge tu, nawe utapata baraka, hatujawahi kukaa na ***kupanga*** vitu vya kufanya, kwa vile sisi si watu wa mipango vile, ila wengi wametubariki kwa kutujumuisha kwa mipango yao. Kweli hatuwezi kufanya mambo makubwa, ila yale madogo kwa upendo, na pia hata kama kazi yenyewe ni tone kwenye bahari, basi tukumbuke kwamba tone moja ndiyo linayofanya bahari iwe.

Zamani tulifikiri kwamba tukiwa na pesa au muda siku moja, tutafanya hili au lile katika shamba la Bwana. Tukajikuta kwamba hakuna siku tulikuwa na pesa kwenye akiba, ni kudunduliza na kukata kila tunapopata mshahara au kutoa mda wetu (kihali na mali). Kitu kikubwa ni kumtegemea Bwana na kuendelea siku kwa siku (consistent).
Shemeji yangu mmoja aliviona vile vikanisa vidogo tukivijenga, alicheka akasema, hivi msingi wake si imara vitaanguka; "Mimi nangoja nijenge kanisa kubwa la dola 50,000 lililo na kituo cha vijana kwenye ghorofa yake (youth center);" alisema. Baada ya miaka 10 alikuja kwangu na kusema, "Nimegundua kwamba hakutafika wakati kama huo, maana pesa inaingia mkononi na kutoweka, afadhali kujenga hivi vibanda vya makanisa kama vyenu!"

Mchungaji mmoja alituita siku moja ili tujenge kanisa kwa wahitaji kule Kigoma. Hatukuwa na uwezo. Akasema, "Je, hamna hata dola 100, tupate wanawake wachote maji na kukandika udongo na kuleta miti, ili niwajengee hawa watu nyumba ya udongo na majani?". Kabla hatujafikiria nyota juu kwenye anga, wacha tufikirie madogo tu yale ambayo Mungu Anatuwezesha kufanya siku kwa siku. Ni nani ajuaye pengine siku moja akatukabidhi hayo makubwa tuyafanye? Hitaji letu kuu ni maombi tafadhali jiunge kuomba nasi ili Bwana atutumie katika shamba Lake. Yeye aliyeaanza kazi njema moyoni mwenu Ataimaliza, ni jambo la kututia moyo katika uwakili wetu. Mwitiko wetu uwe, "Nipo hapa Bwana nitume!". Kwa kifupi tukumbuke kwamba si tu 10% ya vyote tulivyo navyo ndiyo vya BWANA bali 100%.
Nimejiuiliza mara nyingi nitapata wapi uwezo. Na kwa vile nina watoto wadogo, maana nilizaa nikiwa na zaidi ya miaka 40, nimejiuliza sasa nikitoa kwa mtu watoto wangu watasomaje? Hakika ni changamoto kusomesha na tumeanza kazi hii ambayo siyo ndogo. Maana karibu nastaafu na nguvu zinanipungua ila watoto bado wadogo. Siku moja nikitembea mtaa nilioishi kule Jersey City, New Jersey, maili tatu kufikia Manhattan yale majengo marefu yalipopigwa bomu na magaidi. Nilimwona bwana

fulani ana mbwa mkubwa sana mweupe, anayependeza kweli kweli. Nikamkimbilia na kumwuliza mbwa wake ana uzito gani? Akasema kilo 140! Nikashangaa sana, akaendelea kujigamba kwangu “Jibwa hili linakula si mchezo!”. Nikasema kwa mwezi anakula kiasi gani, akasema “natumia dola elfu moja kumlisha kila mwezi!!”. Nilishangaa maana tulikuwa sita ndani ya nyumba, na pengine tulitumia pungufu ya dola 500 kwa mwezi, na huyu mbwa tu anamwendesha hivi. Ndipo jibu likaja moyoni, huyu anapenda mbwa na amemwomba Mungu wake amsaidie kufanikisha mapenzi yake hayo na kuwa na mbwa kipenzi/pet (hobby). Wewe kama unapenda watu mwambie Mungu akusaidie, daima hatakuacha, atakusaidia ili ufanye huduma ya kusaidia watu na kazi ya Mungu. Hebu tusaidiane kuombeana tuwe mawakili wema tushinde uchoyo kabisa. Na pia Mungu atufungulie madirisha ya mbinguni kwani madirisha ndiyo mengi kwenye nyumba kuliko milango!
Je, leo ungeambiwa una masaa 24 tu kuishi, na kesho ungekufa, ungefanya nini kwa haraka? John Wesley alisema nitaishi tu kama navyoishi kila siku naye akatoa ratiba yake ya siku, “Nitaamka asubuhi na kusoma Biblia na kuomba, kisha nitachukua chakula na kumpelekea mama mjane na watoto wake, kisha nitaenda mkutano wa ibada ya asubuhi, kisha nitaenda kulima masaa 2 shambani mwangu, kisha nitaenda kutembelea watu nyumba kwa nyumba na kuzungumza nao kuhusu Injili…..nk”. Daudi asema ‘nimrudishie nini BWANA kwa wema Wake alionitendea?’. Aligundua Mungu ana kila kitu, yaani kinyangarika mimi nitampa nini Mungu? Akaona kilichobakia kwake ni kumshukuru BWANA, na kuwaambia watu wengine mema ya BWANA na yeyé mwenyewe kushika amri za BWANA, na shuhuda Zake.

**<u>MASOMO YA BIBLIA KWA WATOTO</u>**

## NURU GIZANI

*Mch. Msafiri I. Mtenzi*

i

Ukitaka kutumia kitabu hiki wasiliana na Mchungaji Msafiri Mtenzi, mboreshe pamoja utume

***Kwa Maswali na Majibu:***

*Barua pepe: kwelizabiblia@gmail.com*
*Simu: 0755 040766*
*Mbeya - Tanzania.*

Toleo la Kwanza 2022
Kupigwa chapa na:-

ii

---

YALIYOMO

1. Biblia
2. Amri
3. Sanamu
4. Yesu Kristo
5. Ubatizo wa Biblia
6. Sabato ya Bwana
7. Ibada ya Jumapili
8. Dalili za kuja kwa Yesu mara ya pili
9. Kuja kwa Yesu mara ya pili
10. Kunena kwa Lugha
11. Miujiza
12. Kanisa la Mungu
13. Wafu wako wapi?
14. Onyo la Mwisho
15. Hukumu
16. Mwisho wa Dunia
17. Kwanini watu wengi wanapotea wakati Neno la Mungu liko wazi?

---

**1)<u>BIBLIA</u>**

**1. Je? Biblia imepatikanaje?**
**2 Petro 1;21**
"Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu"
**2 Timotheo 3;16**
"Kila Andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa Mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki"
**NB; Biblia imetufikia kwa njia ya uvuvio wa Roho Mtakatifu. Wanadamu walitumiwa na Roho wa Mungu katika kuiandika Biblia.**

**2. Biblia inatusaidiaje watu kizazi hiki?**
**Warumi 15;4**
"Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya Maandiko tupate kuwa na tumaini"

**3. Kazi ya Biblia ni nini kwa Wakristo wote?**
**Zaburi 119;105**
"Neno Lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu"

**2 Wakorintho 5; 14-17**
"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya"
**NB; Biblia ni kiongozi cha pekee kutufikisha katika kiwango cha juu cha kumjua Mungu. Ikipokelewa kwa Imani kwa njia ya Roho Mtakatifu inauwezo wa kubadilisha maisha ya mwanadamu. Kuna ushahidi tele wa watu ambao maisha yao yamebadilika kwa kusoma Maandiko Matakatifu. Hebu jijengee utaratibu wa kusoma Neno la Mungu kila siku na kwa maombi mengi maisha yako yatabadilika.**
**Luka 4; 33- 35**
"Na ndani ya sinagogi mlikuwa na mtu mwenye roho ya pepo mchafu, akalia kwa sauti kuu, akisema, Acha! Tuna nini Nawe, Yesu wa Nazareti? Umekuja kutuangamiza? Nakujua U Nani, Mtakatifu wa Mungu. Yesu Akamkemea, Akisema, Fumba kinywa, mtoke. Ndipo yule pepo akamwangusha katikati, akamtoka asimdhuru neno"

**NB; Zaidi ya kuwa na nguvu za kubadilisha maisha ya mwanadamu, Neno la Mungu pia lina nguvu ya uponyaji. Nguvu hii hii ilitumika katika kuumba ulimwengu na vyote vilivyo ndani yake.**

**4. Kazi nyingine ya Neno la Mungu kwa mwanadamu ni ipi?**
**Yohana 17;17**
"Uwatakase kwa ile Kweli; Neno Lako ndiyo Kweli"

**5. Neno la Mungu litadumu kwa muda gani?**
**Isaya 40;8**

“Majani yakauka, ua lanyauka; Bali Neno la Mungu wetu litasimama milele”

**6. Ili kuielewa Biblia vizuri inabidi kufanya nini?**
**Matendo 17; 11**
“Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea Lile Neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza Maandiko kila siku, waone kwamba Mambo Hayo ndivyo Yalivyo”

**7. Kuna sehemu ya Biblia Ambayo ni ngumu kuielewa?**
**2 Petro 3;15, 16**
“Nanyi uhesabuni uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu, kama vile na ndugu yetu mpenzi Paulo
alivyowaandikia kwa hekima aliyopewa; vile vile kama katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na Maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe”

**8. Kanuni nyingine ya kuielewa Biblia vizuri ni ipi?**
**Isaya 28:10**
“Kwa maana ni Amri juu ya Amri, Amri juu ya Amri; Kanuni juu ya Kanuni, Kanuni juu ya Kanuni; huku kidogo na huku kidogo”
**NB; Ijapokuwa kuna aya ambazo ni ngumu kuzielewa ndani ya Biblia, lakini ikisomwa kwa kulinganisha mstari na mstari, aya kwa aya na hata sura moja hadi nyingine, kwa maombi mengi mwanadamu anaweza kuzijua siri nyingi za muhimu zilizo katika Biblia.**

**9. Je? Tunaye msaidizi na kiongozi katika kusoma Biblia?**
**Yohana 14; 15, 16**

“Mkinipenda, mtazishika Amri Zangu. Nami nitamwomba Baba, Naye atawapa Msaidizi mwingine, ili Akae nanyi hata milele”
**Yohana 16:13**
“Lakini Yeye Atakapokuja, huyo Roho wa Kweli, Atawaongoza Awatie kwenye Kweli yote; kwa maana
hatanena kwa shauri Lake Mwenyewe, lakini yote Atakayoyasikia Atayanena, na mambo yajayo Atawapasha habari Yake”

**10. Tunaweza kumwomba Mungu nini juu ya Neno Lake?**
**Zaburi 119;18**
“Unifumbue macho yangu niyatazame Maajabu yatokayo katika Sheria Yako”
**NB; Wakati mwingi tutalazimika kumwomba Mungu atufumbue macho ili kuyaelewa vizuri Maandiko Matakatifu. Anza kusoma Biblia kila siku ijapo aya chache tu utajikuta baadaye imekuwa mazoea yako kusoma Maandiko.**
**11. Baadhi ya watu wa siku za mwisho watafanya nini na Neno la Mungu?**

**i) Watakataa Mafundisho Yenye uzima**

**2 Timotheo 4:3, 4**
“Maana utakuja wakati watakapoyakataa Mafundisho Yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe
watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo”

**ii) Watayapotosha baadhi ya Maandiko**
**2 Petro 3:16**
“vile vile kama katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na Maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe”

**iii) Watabadilisha baadhi ya Maandiko Matakatifu**
**Danieli 7:25**
“Naye atanena maneno kinyume Chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu Wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na Sheria; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati”

**NB; Katika ulimwengu wa Wakristo leo Maandiko Matakatifu yamepotoshwa hata kubadilishwa. Tunaona mfano Mungu aliagiza watu wamwabudu na kufanya ibada maalumu siku ya kumbukumbu ya uumbaji kila juma katika siku ambayo ni ya saba ya juma (Jumamosi). Cha ajabu ni kuwa Wakristo wengi wanaabudu siku ya kwanza ya juma ambayo ni Jumapili. Badiliko hilo haliidhinishwi na Neno la Mungu. Na wengi wanapoambiwa juu ya mabadiliko haya hukataa na kuendelea kutolitii Neno la Mungu.**

**2)AMRI ZA MUNGU**
**1. Je? Mungu ana Amri Zake?**
**Kutoka 31:18**
“Hapo Bwana Alipokuwa amekwisha zungumza na Musa katika mlima wa Sinai, akampa hizo mbao mbili za ushuhuda, mbao mbili za mawe, zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu”

**2. Wajibu wa mwanadamu ni nini?**
**Mhubiri 12; 13**
“Hii ndiyo jumla ya Maneno; yote yamekwishasikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike Amri Zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu”

**3. Amri hizo ni zipi?**
**Amri ya kwanza (Kutoka 20; 1-3)**
“Mungu akanena Maneno Haya yote akasema, Mimi ni Bwana, Mungu wako, Niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila Mimi”
**Amri ya Pili (Kutoka 20; 4-6)**
“Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho

juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa Mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; Nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, Nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika Amri Zangu"

**Amri ya Tatu (Kutoka 20; 7)**

"Usilitaje bure Jina la Bwana, Mungu wako, maana Bwana Hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye Jina Lake bure"

**Amri ya Nne (Kutoka 20; 8-11)**

"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, Akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana Akaibarikia siku ya Sabato Akaitakasa.

**Amri ya Tano (Kutoka 20; 12)**

"Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako"

**Amri ya Sita (Kutoka 20; 13)**

"Usiue"

**Amri ya Saba (Kutoka 20; 14)**

"Usizini"

**Amri ya Nane (Kutoka 20; 15)**

"Usiibe"

**Amri ya Tisa (Kutoka 20; 16)**

"Usimshuhudie jirani yako uongo"

**Amri ya Kumi (Kutoka 20; 17)**

"Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako"

**4. Je? amri hizi zina mapungufu au zimekamilika?**

**Zaburi 19; 7 (Ni kamilifu na safi)**

"Sheria ya Bwana ni kamilifu, Huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa Bwana ni amini, Humtia mjinga hekima"

**Warumi 7;12 (takatifu na ya haki)**

"Basi Torati ni takatifu, na ile Amri ni Takatifu, na ya haki, na njema"

**Mithali 30; 5, 6 (zimehakikishwa)**

"Kila Neno la Mungu limehakikishwa; Yeye ni ngao yao wamwaminio. Usiongeze neno katika Maneno Yake; Asije Akakulaumu, ukaonekana u mwongo. Usiongeze neno katika Maneno Yake; Asije akakulaumu, ukaonekana u mwongo"

**5. Je? wanadamu wanaruhusa ya kubadili Amri za Mungu au kuongeza neno lolote?**

**Zaburi 89:34 (Mungu hawezi kuibadilisha)**

"Mimi sitalihalifu Agano Langu, Sitalibadili Neno lililotoka midomoni Mwangu"

**6. Mathayo 5; 17-19 (Yesu hakuja kuibadilisha)?**
"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua Torati au Manabii; la, Sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, Basi mtu ye yote atakayevunja Amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni"

**7. Je? Biblia ilitabiri kuwa Amari za Mungu zitabadilishwa?**
**Danieli 7:25**
"Naye atanena maneno kinyume Chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu Wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na Sheria; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati"

**8. Biblia inasema nini zaidi juu ya kubadilishwa Amri?**
**Isaya 24:5**
"Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi Sheria, wameibadili Amri, wamelivunja Agano la milele"

**9. Je? Biblia inakataza kutengeneza sanamu na kuziabudu?**
**Kutoka 20; 4-6**
"Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa Mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu Mwenye wivu; Nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, Nami Nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika Amri Zangu"

**10. Kwanini Biblia inakataza kutengeneza na kuabudu sanamu?**
**Zaburi 115:4-9**
"Sanamu zao ni fedha na dhahabu, Kazi ya mikono ya wanadamu. Zina vinywa lakini hazisemi, Zina macho lakini hazioni, Zina masikio lakini hazisikii, Zina pua lakini hazisikii harufu, Mikono lakini hazishiki, miguu lakini haziendi, Wala hazitoi sauti kwa koo zake. Wazifanyao watafanana nazo, Kila mmoja anayezitumainia. Enyi Israeli, mtumainini Bwana; Yeye ni msaada wao na ngao yao"

**NB; Neno la Mungu linakataza kutengeneza na kuabudu sanamu. Kwa sababu hazina msaada wowote kwa Mkristo. Mungu Anasema wanaozitengeneza na kuziabudu watafanana nazo watakuwa hawa sikii wala kuzingatia Neno la Mungu. Wakristo inabidi turudi katika Neno la Mungu na kumwomba kwa msaada Wake tuanze kumtii Mungu, katika makanisa mengi sanamu zipo lakini Mungu anakataza jambo hilo katika Amri Zake kumi na kwenye Biblia yote kwa ujumla.**

**11. Mungu Ameagiza nini juu siku ya kuabudu?**
**Kutoka 20; 8-11**
"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye

kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana Akaibarikia siku ya Sabato Akaitakasa.

**12. Kosa kubwa la Wakristo wa leo ni lipi?**
**Isaya 58:1, 13**
"Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao. Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu Wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku Takatifu ya Bwana Yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutozifanya njia zako wenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe"

**NB; Kosa kubwa la wakristo wa leo ni kutoabudu siku ya Sabato, kufanya anasa siku ya Sabato na hata kutotunza kabisa Sabato. Sabato ni siku ya saba ya juma ambayo ni Jumamosi. Siku hizi wakristo wengi wanatunza siku ya kwanza ya Juma ambayo ni Jumapili badala ya siku ya Sabato. Mungu anatia shime watu wa Mungu ikiwa ni pamoja na Wachungaji kuwaambia Wakristo juu ya kosa lao kubwa la kutotunza siku ya Sabato ambayo ni Jumamosi. Kwa hakika ibada ya Jumapili siyo Agizo la Mungu kwani hata Bwana Yesu aliabudu siku ya saba ya juma ambayo ni Jumamosi.**

**13. Ni sababu ipi inatolewa kwa Wakristo kuabudu siku ya kwanza ambayo ni Jumapili?**

**NB; Wanasema kuwa Bwana Yesu Alifufuka siku hiyo. Sababu hii haina msingi katika Maandiko Matakatifu, kwani Yesu baada ya kufufuka Alikaa duniani siku 40 lakini katika siku zote hizo hakuagiza kuwa sasa watu wanaweza kuabudu siku ya kwanza yaani Jumapili au yoyote ile isipokuwa Sabato ya Bwana. Yeye Alisema (Luka 16:17, "Lakini ni vyepesi zaidi mbingu na nchi vitoweke, kuliko itanguke nukta moja ya Torati") na Mungu pia Alisema, (Zaburi 89:34, "Mimi sitalihalifu Agano Langu, Sitalibadili Neno lililotoka midomoni Mwangu"). Mpendwa umeona wazi kabisa kuwa, Biblia haikubaliani na badiliko la siku ya kuabudu toka siku ya Saba (Jumamosi) hadi siku ya kwanza (Jumapili). Ni vizuri uamue toka sasa kuanza kuabudu siku ya Sabato ya Jumamosi.**

**14. Kama unaabudu siku ya Jumapili badala ya Sabato (Jumamosi) unakuwa unatii Amri kumi? Na kosa lako linakuwa lipi?**
**Yakobo 2; 10,11**
"Maana mtu awaye yote atakayeishika Sheria yote, ila akajikwaa katika Neno moja, amekosa juu ya yote. Kwa maana Yeye aliyesema, Usizini, pia Alisema, Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja Sheria"

**15. Moja kati ya masharti ya kuingia mbinguni ni lipi?**
**Mathayo 19:16, 17**
"Na tazama, mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele? Akamwambia Kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike Amri"

**16. Je? neema inaondoa umuhimu wa Amri kumi za Mungu?**
**Tito 2; 11,12**
"Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa"

**17. Watakatifu wa siku za mwisho watafanya nini?**
**Ufunuo 14:12**
"Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao Amri za Mungu, na imani ya Yesu".

**18. Mungu anaswali moja tu analokuuliza mpendwa msomaji.**
**Kutoka 16:26-28**
"Siku sita mtaokota; lakini siku ya saba ni Sabato, siku hiyo hakitapatikana. Ikawa siku ya saba wengine wakatoka kwenda kukiokota, wasikione. Bwana Akamwambia Musa, Mtakataa kuyashika Maagizo Yangu na Sheria Zangu hata lini?

**19. Je? Amri ziliishia msalabani?**
**a) Zaburi 89:34**
"Mimi sitalihalifu Agano Langu, Sitalibadili Neno lililotoka midomoni Mwangu"
**NB; Mungu Anasema hataweza kuligeuza Neno lilotoka midomoni Mwake.**
**b) Warumi** 7;12
"Basi Torati ni Takatifu, na ile Amri ni Takatifu, na ya haki, na njema"
**NB; Miaka mingi baada ya msalaba Mtume Paulo anasema Amri ni Takatifu na Njema.**
**c) Luka 16:17**
"Lakini ni vyepesi zaidi mbingu na nchi vitoweke, kuliko itanguke nukta moja ya Torati"
**NB; Mbingu bado hazijatoweka, hivyo amri bado zipo.**
**d) Ufunuo 14:12**
"Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao Amri za Mungu, na imani ya Yesu"

**20. Biblia inasema nini zaidi juu ya amri?**
i) **Yohana 14:15 (tukimpenda Yesu tutashika Amri za Mungu)**
"Mkinipenda, mtazishika Amri Zangu"
ii) **1 Yohana 5:3 (kumpenda Mungu ni kushika Amri Zake)**

“Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike Amri Zake; wala Amri Zake si nzito”

**iii) 1Yohana 2:4 (ukisema unamjua Mungu lakini hushiki Amri Zake unakuwa mwongo)**

“Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki Amri Zake, ni mwongo, wala Kweli haimo ndani yake”

**21. Je? Sanduku la Agano, lilionekana mbinguni miaka mingi baada ya msalaba?**

**Ufunuo 11:19**

“Kisha Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na sanduku la Agano Lake likaonekana ndani ya hekalu Lake. Kukawa na umeme, na sauti, na radi, na tetemeko la nchi, na mvua ya mawe nyingi sana.

**22. Kuna madhara yoyote walimwengu wanapobadilisha na wanapovunja Amri za Mungu?**

**Isaya 24:3-6**

“Dunia hii itafanywa tupu kabisa, na kuharibiwa kabisa; maana Bwana Amenena Neno Hilo. Dunia inaomboleza, inazimia; ulimwengu unadhoofika, unazimia; watu wakuu wa dunia wanadhoofika. Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi Sheria, wameibadili Amri, wamelivunja Agano la milele. Ndiyo sababu laana imeila dunia hii, na hao wanaoikaa wameonekana kuwa na hatia, ndiyo sababu watu wanaoikaa dunia wameteketea, watu waliosalia wakawa wachache tu.

**Isaya 24:19,20**

“Dunia kuvunjika, inavunjika sana; dunia kupasuka, imepasuka sana; dunia kutikisika, imetikisika sana. Dunia inalewa-lewa kama mlevi, nayo inawaya-waya kama machela; na mzigo wa dhambi zake utailemea; nayo itaanguka, wala haitainuka tena.

**3)<u>SANAMU</u>**

**1. Je? Mungu alikataza ibada ya sanamu katika Agano la kale?**

**Walawi 26:1**

“Msifanye sanamu yo yote, wala msijisimamishie sanamu ya kuchonga, wala mnara,
wala msiweke jiwe lolote lililochorwa katika nchi yenu ili kulisujudia; kwa kuwa Mimi Ndimi Bwana, Mungu wenu”

**NB; Tangu zama za kale uchongaji na utengenezaji sanamu kwaajili ya kuabudu ulikataliwa na Mungu vikali sana.**

**2. Je? wana wa Israeli waliwahi kufanya sanamu?**

**Kutoka 32:4**

“Akaipokea mikononi mwao akaitengeneza kwa patasi, akaifanya iwe sanamu ya ndama kwa kuiyeyusha; nao wakasema, Hiyo ndiyo miungu yako, Ee Israeli, iliyokutoa katika nchi ya Misri”

**3. Biblia inasema nini zaidi kuhusu sanamu?**
**Kumbukumbu la Torati 7:5,6**
"Lakini watendeni hivi; zivunjeni madhabahu zao zibomosheni nguzo zao, yakateni maashera yao, ziteketezeni kwa moto sanamu zao za kuchonga. Kwa maana wewe u taifa Takatifu kwa Bwana, Mungu wako; Bwana Mungu wako, Amekuchagua kuwa watu Wake hasa, zaidi ya mataifa yote walioko juu ya uso wa nchi.
**Kumbukumbu la Torati 4:15-17**
"Jihadharini nafsi zenu basi; maana hamkuona umbo la namna yo yote siku ile Bwana Aliyosema nanyi kutoka kati ya moto; msije mkajiharibu nafsi zenu, mkajifanyia sanamu ya kuchonga, mfano wa sura yo yote, mfano wa mwanamume au mwanamke, mfano wa mnyama yeyote aliye duniani, au mfano wa ndege ye yote arukaye mbinguni"
**Kumbukumbu la Torati 27:15**
"Na alaaniwe mtu afanyaye sanamu ya kuchonga, au ya kusubu, machukizo kwa Bwana, kazi ya mikono ya fundi, akaisimamisha kwa siri. Na watu wote wajibu, waseme, Amina"
**Zaburi 97:6, 7**
"Mbingu zimetangaza haki Yake, Na watu wote wameuona utukufu Wake. Na waaibishwe wote waabuduo sanamu, Wajivunao kwa vitu visivyofaa; Enyi miungu yote, msujuduni Yeye.

**4. Mungu Aliwafanya nini watu waliotengenza na kuabudu sanamu?**
**Kutoka 32:35**
"Bwana akawapiga hao watu, kwa walivyoifanya ile ndama, ambayo Haruni aliifanya"
**NB; Bwana Mungu Aliwaadhibu watengeneza na waabudu sanamu.**

**5. Kuonyesha kuwa Mungu hapendi sanamu Alitoa Amri gani?**
**Kumbu kumbu 7:25**
"Sanamu za kuchonga za miungu yao *mtaziteketeza kwa moto*; usitamani fedha wala dhahabu iliyo juu yao, wala usiitwae iwe yako usije ukanaswa nayo; kwa maana ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako".

**6. Je? Ipo Amri inayokataza kutengeneza, kuitumikia na kuibadu sanamu miongoni mwa Amri kumi za Mungu?**
**Kutoka 20:4-6**
"Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa Mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; Nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, Nami Nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika Amri Zangu"

**NB; Neno la Mungu liko wazi kabisa juu ya kutengeneza kuchonga sanamu kwaajili ya kuabudu. Lakini pia inajumuisha kuitumikia sanamu. Mungu**

**Anasema sanamu isingetengenezwa kwa mfano wa kitu chochote, si mwanawe Yesu Kristo, msalaba wa Yesu wala watakatifu wa kale au kitu chochote kile. Lakini cha kushangaza katika ulimwengu wa Wakristo leo sanamu zinaonekana katika makanisa. Lakini Ukweli unabakia pale pale, ya kwamba Mungu anakataza utengenezaji na uabuduji wa sanamu.**

**7. Je? Mitume katika Agano jipya walipambana na upinzani toka kwa waabudu sanamu?**
**Matendo 19:24-29**
"Kwa maana mtu mmoja, jina lake Demetrio, mfua fedha, aliyekuwa akifanya vihekalu vya fedha vya Artemi, alikuwa akiwapatia mafundi faida nyingi. Akawakusanya hao, pamoja na wengine wenye kazi ile ile, akasema, Enyi wanaume, mnajua ya kuwa utajiri wetu hutoka katika kazi hii. Tena mnaona na kusikia ya kwamba si katika Efeso tu, bali katika Asia yote pia Paulo huyo ameshawishi watu wengi na kuwageuza nia zao, akisema ya kwamba hiyo inayofanywa kwa mikono siyo miungu. Si kwamba kazi hii yetu ina hatari ya kudharauliwa tu; bali na hekalu la mungu mke aliye mkuu, Artemi, kuhesabiwa si kitu, na kuondolewa utukufu wake, ambaye Asia yote pia na walimwengu wote humwabudu. Waliposikia haya wakajaa ghadhabu, wakapiga kelele, wakisema, Artemi wa Waefeso ni mkuu. Mji wote ukajaa ghasia, wakaenda mbio wakaingia mahali pa michezo kwa nia moja, wakiisha kuwakamata Gayo na Aristarko, watu wa Makedonia waliosafiri pamoja na Paulo.

**8. Je? Sanamu ina msaada wowote kwa anayeiabudu?**
**Zaburi 135:15-18**
"Sanamu za mataifa ni fedha na dhahabu, Kazi ya mikono ya wanadamu. Zina vinywa lakini hazisemi, Zina macho lakini hazioni, Zina masikio lakini hazisikii, Wala hamna pumzi vinywani mwake. Wazifanyao watafanana nazo, Na kila mmoja anayezitumainia"

**9. Kwanini Mungu anakataza watu wasifanye sanamu ili kuziabudu?**
**Kutoka 20:5**
"Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa Mimi, Bwana, Mungu wako, ni ***Mungu Mwenye wivu;*** Nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao".

**10. Nini tunaweza kufanya ikiwa sanamu zipo katika makanisa yetu?**
**1 Wakorintho 10:14**
**"**Kwa ajili ya hayo, wapenzi wangu, ikimbieni ibada ya sanamu".

**11. Kitu kingine kinachoweza kuwachochea watu wafanye sanamu ni nini?**
**Matendo 19:26, 27**
"Tena mnaona na kusikia ya kwamba si katika Efeso tu, bali katika Asia yote pia Paulo huyo ameshawishi watu wengi na kuwageuza nia zao, akisema ya kwamba hiyo inayofanywa kwa mikono siyo miungu. Si kwamba kazi hii yetu ina hatari ya kudharauliwa tu; bali na hekalu la mungu mke aliye mkuu, Artemi, kuhesabiwa si kitu, na kuondolewa utukufu wake, ambaye Asia yote pia na walimwengu wote

humwabudu.

**12. Je? sanamu za Yesu au watakatifu zinakubalika katika nyumba ya ibada?**
**Kutoka 20:4-6**
"Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa Mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu Mwenye wivu; Nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha Wanichukiao, Nami Nawarehemu maelfu elfu Wanipendao, na kuzishika Amri Zangu".

**13. Je? waabudu sanamu wataingia mbinguni?**
**1 Wakorintho 6:9**
"Au hamjui ya kuwa wadhalimu **hawataurithi ufalme wa Mungu?** Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti"
**Ufunuo 21:8**
"Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili"

**14. Mimi kama Mkristo wajibu wangu ni upi?**
i) **Kumtii Mungu na kuzishika Amri Zake,**
**Mhubiri 12:13**
"Hii ndiyo jumla ya Maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike Amri Zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu"
**ii) Kumpenda Yesu na kuzitii Amri Zake**
**Yohana 14:15**
"Mkinipenda, mtazishika Amri Zangu"
**iii) Kuikimbia ibada ya sanamu**
**1 Wakorintho 10:14**
"Kwa ajili ya hayo, wapenzi wangu, ikimbieni ibada ya sanamu"
**NB; Kitu cha muhimu ambacho Mkristo anapaswa kuzingatia katika siku hizi za mwisho ni kusoma Maandiko ili kujua Mungu Anataka tufanye nini, mafundisho ya uongo yametapakaa kila mahali. Bila kusoma Maandiko kwa maombi mengi wengi watapotea milele. Huu sio wakati wakuwatumainia wachungaji tu, bali kusoma Biblia kwa maombi mengi.**

## 4)YESU KRISTO

**1. Yesu Kristo ni nani?**
**Je? Alikuwepo kabla ya kuzaliwa?**
**Yohana 8:58**
"Yesu akawaambia, Amin, amin, Nawaambia, yeye Ibrahimu asijakuwako, Mimi Niko"
**Isaya 9:6,7**
"Maana kwa ajili yetu mtoto Amezaliwa, Tumepewa Mtoto Mwanamume; Na

uweza wa kifalme utakuwa begani Mwake; Naye ataitwa Jina Lake, Mshauri wa ajabu, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani" Maongeo ya enzi Yake na amani Hayatakuwa na mwisho kamwe, Katika kiti
cha enzi cha Daudi na ufalme Wake; Kuuthibitisha na kuutegemeza Kwa hukumu na kwa haki, Tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo.

**2. Hii ni kweli?**
**Hesabu 23:19**
"Mungu si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena, hatalifikiliza?

**3. Alikuja ulimwenguni kufanya nini?**
**Yohana 10:10**
"Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; Mimi Nalikuja, Ili wawe na uzima kisha wawe nao tele.

**4. Je? Yesu aAitabiriwa ndani ya Biblia kabla ya kuja Kwake?**
**Mahali pa kuzaliwa**
**Mika 5:2**
"Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe
Atanitokea Mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo Yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele"
**Atazaliwa na nani?**
**Isaya 7:14**
"Kwa hiyo Bwana Mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa Mtoto mwanamume, Naye atamwita Jina Lake Imanueli"
**Kazi Yake**
**Isaya 61:1**
"Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu Bwana Amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; Amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao"
**Kifo Chake**
**Zaburi 22:18**
"Wanagawanya nguo Zangu, Na vazi Langu wanalipigia kura"

**5. Zawadi Yake kuu kwa mwanadamu ni ipi?**
**Yohana 3:16**
"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu Amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele"

**NB; Kuutoa uhai Wake kwaajili ya mwanadamu aliyepotea ilikuwa ni zawadi kubwa sana ambayo Mungu aliutolea ulimwengu. Zawadi hii ingekuwa na manufaa pale tu ambapo mwanadamu anapomkili Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wake.**

**6. Je? Yesu Kristo alikuwa mtiifu kwa Baba Yake?**
**Yohana 15:10**
"Mkizishika Amri Zangu, mtakaa katika pendo Langu; kama vile Mimi Nilivyozishika Amri za Baba Yangu na kukaa katika pendo Lake"

**7. Je ? Bwana Yesu aliabudu siku gani?**
**Luka 4:16**
"Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya Sabato Akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi Yake, Akasimama ili asome"

**8. Kwanini Yesu Alikufa msalabani?**
**Yohana 3:16, 17**
"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata Akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu Amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika Yeye.
**Yohana 12:32**
"Nami Nikiinuliwa juu ya nchi, Nitawavuta wote Kwangu"

**9. Kabla ya kuondoka aliahidi nini?**
**Yohana 14:1-3**
"Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na Mimi. Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi; kama sivyo, Ningaliwaambia; maana Naenda kuwaandalia mahali Basi Mimi Nikienda na kuwaandalia mahali, Nitakuja tena iwakaribishe Kwangu; ili Nilipo Mimi, nanyi mwepo"

**10. Je? Yesu Atakuja tena? Kufanya nini?**
**Yohana 14:3**
"Basi Mimi Nikienda na kuwaandalia mahali, Nitakuja tena niwakaribishe Kwangu; ili Nilipo Mimi, nanyi mwepo"

**11. Je? Yesu Anatoa wito gani?**
**Ufunuo 3:20, 21**
"Tazama, Nasimama mlangoni, Nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango Nitaingia kwake, Nami Nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami. Yeye ashindaye, Nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi, kama Mimi Nilivyoshinda Nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi"
**NB. Yesu Amesimama katika mlango wa moyo wako Anabisha hodi, ni jambo zuri kumkaribisha ili aingie na kubadilisha maisha yako. Atakufanya kuwa mtu mpya.**

## 5)UBATIZO WA BIBLIA

**1. Je? ubatizo ni lazima kwaajili ya kuingia kwenye ufalme wa Mungu?**
**Marko 16;16**
"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa"

**2. Je? ubatizo ni Agizo la Yesu?**
**Mathayo 28; 19-20**
"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana,
na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari"

**3. Je? Yesu Mwenyewe alituachia kielelezo cha kubatizwa.**
**Mathayo 3; 16-17**
"Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunuka, Akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu Yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, Mpendwa Wangu, Ninayependezwa Naye"

**4. Kuna aina ngapi za Ubatizo?**
**Waefeso 4:5**
"Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja"

**5. Je? hiyo aina moja ni ipi?**
**Mathayo 3; 16-17**
"Naye Yesu Alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia,akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu Yake; na tazama,
sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, Ninayependezwa Naye"
**Yohana 3:23**
"Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni karibu na Salimu, kwa sababu huko kulikuwa na maji tele; na watu wakamwendea, wakabatizwa.
**NB; Aina moja inayokubaliwa na Neno la Mungu ni ile ya kubatizwa ndani ya maji mengi, ndiyo maana Yohana alienda Ainoni kulikokuwa na maji mengi.**

**6. Unapobatizwa kwa Ubatizo huu Mungu Anasemaje?**
**Mathayo 3:17**
"…. na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, Mpendwa Wangu, Ninayependezwa Naye.
**NB; Katika ulimwengu wa Kikristo leo, kuna aina nyingi za ubatizo. Miongoni mwa aina zinatumika sana ni ule wa kubatiza kwa kuzamisha ndani ya maji ambao huo unaagizwa katika biblia. Lakini aina nyingine kama ule wa kunyunyazia maji kichwani, au wa kuruka moto au ule wa kuchora msalaba katika uso, aina hizi hazikuagizwa na Neno la Mungu.**

**Kwa hiyo, aina ni moja tu inayotambuliwa na Maandiko Matakatifu yaani wa kuzamisha mwili wote ndani ya maji mengi. Biblia inatushauri kufuata kielelezo cha Yesu cha kubatizwa kwa kuzamisha ndani ya maji mengi.**

**7. Mkristo wa leo aliye mwaminifu kwa Mungu wake angepaswa kubatizwa namna gani?**
**1 Petro 2:21**
"Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo Naye Aliteswa kwa ajili yenu, Akawaachia kielelezo, mfuate nyayo Zake"
**NB; Mkristo wa leo anapaswa kufuata nyayo za Yesu na kubatizwa kwa kuzamishwa ndani ya maji mengi. Vinginevyo anakuwa hampendi wala hamtii Yesu. (Yohana 14;15, Yesu Anasema mkinipenda mtazishika Amri Zangu)**

**8.Je? ubatizo una masharti yoyote?**
**Sharti la kwanza kujifunza (Mathayo 28:19)**
"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu"
**Sharti la pili: Kuamini. (Marko 16; 16)**
"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa"
**Sharti la tatu: Kutubu. (Matendo 3: 19)**
"Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako Kwake Bwana"
**Sharti la Nne: Kubatizwa kwa maji mengi. (Yohana 3:23)**
"Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu huko kulikuwa na maji tele; na watu wakamwendea, wakabatizwa"

**9. Je? ukishatimiza masharti yote, Je, ni vizuri kukawia kubatizwa?**
**Matendo 8; 36-38.**
"Wakawa wakiendelea njia, wakafika mahali penye maji. Yule towashi akasema tazama maji haya ninini kinachonizuia nisibatzwe. Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote, inawezakana, akajibu akanena, naamni ya kwamba Yesu Kristo Ndiye mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame, wakateremka wote wawili majini. Filipo na yule towashi naye akambatiza"
**NB; Unapokuwa umetimiza masharti yote ya ubatizo si vizuri kukataa au kuchelewa kubatizwa. Ni vema kubatizwa.**

**10. Je? Biblia inasema nini juu ya kubatiza watoto wachanga?**
**Mathayo 19: 13-15**
"Ndipo akaletewa watoto wadogo ili aweke mikono Yake juu yao na kuwaombea; wanafunzi Wake wakawakemea. Lakini Yesu Akasema, Waacheni watoto wadogo waje Kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao. Akaweka mikono Yake juu yao, Akatoka huko"

**11. Kwa nini Yesu hakuagiza watoto wachanga?**
Ni vigumu kuwafundisha watoto wachanga kwani hawataelewa chochote

Watoto wachanga hawawezi kuamini kwa kuwa hawajui mema na mabaya vyema bado.
Pia hawana jambo la kutubu na wala hawajui maana ya kutubu. Kwa ujumla Biblia haiagizi kubatiza watoto wachanga.
**NB: Kama tunampenda Mungu tutafuate Maagizo na Masharti Yake yote kwa neema Yake. Maagizo haya ameyaweka iliyatuongoze Kwenda sawasawa na Mapenzi Yake. Yafaa kila wakati tupate muda wa kusoma Maandiko Matakatifu sisi wenyewe ili tuone anataka tufanye nini?**

**12. Ubatizo unaonyesha ishara gani au una simama badala ya nini?**
**Warumi 6; 5, 6**
"kwa maana kama mlivyounganika Naye katika mfano wa mauti Yake kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka Kwake. Mkijua Neno Hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja Naye ilimwili wa dhambi ubadilike tusitumikie dhambi tena"
**NB; Ubatizo ni mfano wa kufa pamoja na Yesu. Na kufufuka naye tukiwa watu wapya.**

**13. Je? mtu anaweza kubatizwa mara ya pili?**
**Matendo 19:1-5**
"Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika Efeso; akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko; akawauliza, Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia. Akawauliza, Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema, Kwa ubatizo wa Yohana. Paulo akasema, Yohana alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini Yeye takayekuja nyuma Yake, yaani, Yesu. Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu".

**15. Mtu anaruhusiwa kumzuia mtu aliyetayari kwa Ubatizo asibatizwe?**
**Matendo 10:47-48**
"Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa Jina Lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha"
**NB; Neno la Mungu haliruhusu mtu awaye yote kumzuia mtu asibatizwe ambaye ametimiza masharti yote ya kubatizwa. Si baba, mama, ndugu na jamaa au hata viongozi wa dini au serikali.**

**16. Tatizo la Wakristo wa leo ni nini?**
**Marko 7:6 -9**
"Akawaambia, Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, Watu hawa huniheshimu kwa midomo Ila mioyo yao iko mbali Nami; Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu, Ninyi mwaiacha Amri ya Mungu, na kuyashika mapokeo ya wanadamu. Akawaambia, Vema! Mwaikataa Amri ya Mungu mpate kuyashika mapokeo yenu"
**NB; Tatizo la watu wa siku hizi, hawajisomei Neno la Mungu wenyewe. Wanategemea kuambiwa tu na wachungaji, jambo ambalo linafanya wakose kujua Mapenzi ya Mungu. Kila mtu anapaswa kusoma Neno la**

**Mungu, kujua Mungu Anataka nini, na kisha kutenda yalio Mapenzi ya Mungu.**
**Matendo 17:11**
"Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea Lile Neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza Maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo"

## 6)<u>SABATO YA BWANA</u>

**Ijumaa, Jumamosi na Jumapili Ipi ni sabato ya Kweli ?**
**1. Je? Mungu Anayo siku Yake ambayo anataka watu wa mwabudu katika siku hiyo?**
**Kutoka 20:10**
"Lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako,wala mjakazi wako, wala mnyama wako wakufuga, wala Mgeni aliye ndani ya malango yako".

**2. Siku hiyo iliianzishwa wakati gani?**
**Mwanzo 2:1-3**
"Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. Na siku ya saba Mungu Alimaliza kazi Yake yote Aliyoifanya; Akastarehe siku ya saba, Akaacha kufanya kazi Yake yote Aliyoifanya. Mungu Akaibarikia siku ya saba, Akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu Alistarehe, Akaacha kufanya kazi Yake yote Aliyoiumba na kuifanya"

**3. Je? Sabato ni ya nani? ni ya wayahudi kama wengi wanavyodhani?**
**Kutoka 20:10**
"Lakini siku ya sabaini Sabato ya Bwana, Mungu wako,"

**4. Je ? Mungu alimpa nani siku hiyo ?**
**Ezekieli 20:12**
"Tena Naliwapa Sabato Zangu, ziwe isharakati ya Mimi nawao, wapatekujua ya kuwa Mimi, Bwana, Ndimi Niwatakasaye.
**Marko 2:27**
"Akawaambia, Sabato ilifanyika kwaajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya Sabato."
**NB; Biblia inaonyesha wazi kuwa, Sabato sio tu ya wayahudi bali ni watu wote. Sabato ilikuwapo hata wakati wayahudi hawajakuwa.**

**5. Agizo gani limetolewa kuhusu utendaji kazi katika siku hii ?**
**Kutoka 20:10**
"lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako"
**NB; Kazi zinazoweza kutendeka siku ya Sabato ni zile kazi njema**

**zinazohusiana na kuokoa maisha.**

**6. Kwanini Mungu Anakataza watu wasifanye kazi siku ya Sabato?**
**Kutoka 20:11**
"Maana, kwa siku sita Bwana Alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, Akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato Akaitakasa"
**NB; Siku ya Sabato ni siku maalum ya kufanya ibada na kukumbuka kuwa Mungu Ndiye muumba wetu. Mawazo yetu yapaswa yaelekezwe kwa muumba wetu.**

**7. Sabato ilitolewa kama kitambulisho kati ya Mungu na watu Wake?**
**Ezekieli 20:12**
"Tena naliwapa Sabato Zangu, ziwe ishara kati ya Mimi na wao, wapate kujua ya kuwa Mimi, Bwana, Ndimi Niwatakasaye."
**8. Manabii walifundisha juu ya Sabato?**
**Isaya 58:13**
"Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu Wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe"

**9. Je? Yesu Alitunza Sabato?**
**Luka 4:16**
"Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya Sabato Akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi Yake, Akasimama ili asome."
**Yohana 15:10**
"Mkizishika Amri Zangu, mtakaa katika pendo Langu; kama vile Mimi Nilivyozishika Amri za Baba Yangu na kukaa katika pendo Lake."
**NB: Ikiwa Yesu Kristo Bwana wetu Aliweza kumwabudu Mungu siku ya Sabato ingelikuwa wazo zuri na sisi kufuata nyayo Zake kwa kutii Amri za Mungu na kutii Sabato ya Jumamosi na sio Jumapili. Biblia inasema Yesu alishika Amri za Mungu.**

**10. Je? Mitume walitunza Sabato?**
**Mdo 17:2**
"Na Paulo, kama ilivyo kuwa desturi yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa Maneno ya Maandiko Sabato tatu,"

**11. Je ? Sabato ni Amri ya Mungu katika Amri Zake ?**
**Kutoka 20:8-11**
"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sitafanyakazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya sabaini Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala Mgeni aliyendani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana Alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana Akaibarikia siku ya

Sabato Akaitakasa."

**12. Yesu Anasema nini juu ya Amri za Mungu ikiwemo Sabato?**
**Yohana 14:15**
"Mkinipenda, mtazishika Amri Zangu."

**13. Je? Sabato iliishia msalabani au ipo hata leo ?**
**Mathayo 5 :17-18**
"Msidhani nilikuja kuharibu Torati ao Manabii, sikukuja kuharibu, lakini kutimiliza. Kwa maana Kweli Ninawaambia nyinyi mbingu na nchi zitakapoondoka yodi moja wala nukta moja haitoondoka, hata yote yatimie."
**Waebrania 4:9,11**
"Basi, imesalia raha ya Sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana Yeye Aliyeingia katika raha Yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu Alivyostarehe katika kazi Zake. Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo
wa kuasi"
**Isaya 66:22,23**
"kama vile mbingu mpya na nchi mpya, Nitakazofanya zitakavyokaa mbele Zangu, Asema Bwana, ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa.Na itakuwa, mwezi mpya mwezi mpya, Sabato hata Sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele Zangu, Asema Bwana.
**NB; Sabato haikuishia Msalabani, miaka mingi baada ya msalaba Paulo anasema imesalia raha ya Sabato kwa watu wa Mungu. Na pia Mitume walitunza Sabato hata baada ya msalaba.**

**14. Basi Sabato ni siku gani katika juma? Matukio ya wakati wa kifo cha Yesu yanaweza kutuelekeza**
**kutambua juu ya Sabato kuwa ni siku gani?**
**Luka 23:46,47**
"Yesu akalia kwa sauti kuu, Akasema, Ee Baba, mikononi Mwako Naiweka Roho Yangu. Alipokwisha kusema hayo Alikata Roho"
**NB; Sote twajua kuwa Yesu Alikufa siku ya Ijumaa (Wakristo wengi siku hiyo huiita Ijumaa kuu)**
**Luka 23:53-56.**
"Akaushusha, akauzinga sanda ya kitani, akauweka katika kaburi lililochongwa mwambani, ambalo hajalazwa mtu bado ndani yake. Na siku ile ilikuwa siku ya Maandalio, na Sabato ikaanza kuingia" Na wale wanawake waliokuja naye toka Galilaya walifuata, wakaliona kaburi, na jinsi mwili Wake
ulivyowekwa. Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. Na *siku ya Sabato walistarehe* kama ilivyoamriwa.

**NB; Sote tunajua kuwa Yesu alizikwa na Yusufu siku ya maandalio ambayo ni ijumaa. (Ijumaa ni siku ya maandalio ya Sabato kulingana na Biblia). Kwa hiyo, Yesu Alikufa na kuzikwa siku ya maandalio ambayo ni Ijumaa. Siku iliyofuata baada ya maandalio ni Sabato ambayo wanawake walipumzika kama ilivyokuwa kawaida yao. Tunajua wazi kuwa baada**

**ya Ijumaa inafuata Jumamosi, kumbe basi Jumamosi ndio siku ya Sabato ambayo Mungu ameagiza watu wapumzike.**

**Luka 24:1-3, 6**

"Hata siku ya kwanza ya juma, ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini, wakiyaleta manukato waliyoweka tayari. Wakalikuta lile jiwe limevingirishwa mbali na kaburi, wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu"

**Luka 24:6**

"Hayupo hapa, Amefufuka. Kumbukeni Alivyosema nanyi Alipokuwa Akaliko Galilaya"

**NB; Kulingana na matukio haya makuu matatu ( kufa, kuwa kaburini na kufufuka), tunaona kuwa, Yesu Alikufa siku ya maandalio ya Sabato ambayo ni siku ya Ijumaa. Siku iliyofuata baada ya maandalio ni Sabato, Siku hiyo alikuwa kaburini na siku ya kwanza ya juma Yesu Alifufuka, na sote tunajua kuwa Yesu Alifufuka siku ya Jumapili ambayo Biblia inaiita siku ya kwanza ya juma. Hivyo basi Ijumaa ni siku ya sita ya juma, Jumamosi ni siku ya saba ya juma na Jumapili ni siku ya kwanza ya Juma. Ni uamuzi wako ndugu msomaji, kutunza siku ya saba ya Juma ambayo ni Jumamosi au kutunza Jumapili na Ijumaa siku ambazo hazikuagizwa na Mungu. (Yoshua 24:15, Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia Bwana, chagueni hivi leo mtakayemtumikia;...... lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana).**

## 7)IBADA YA JUMAPILI

**1. Zipo siku ngapi ambazo Mungu amezitenga maalumu kwaajili ya kupumzika na kufanya ibada Yake Takatifu?**

**Kutoka 20:8-11**

"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana Alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, Akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana Akaibarikia siku ya Sabato Akaitakasa.

**NB; Mungu Ametenga siku moja tu kwaajili ya kumwabudu Yeye na kupumzika. Na siku hiyo ni siku ya saba ya Juma (Sabato) ambayo ni Jumamosi.**

**2. Je? Jumapili ni siku ya ibada Kulingana na Maandiko Matakatifu?**

**Mwanzo 2:1-3**

"Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi Yake yote Aliyoifanya; Akastarehe siku ya saba, Akaacha kufanya kazi Yake yote Aliyoifanya. Mungu Akaibarikia siku ya saba, Akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu Alistarehe, Akaacha kufanya kazi Yake yote Aliyoiumba na kuifanya.

**Mwanzo 1:3-5**

"Mungu Akasema, Iwe nuru; ikawa nuru. Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni

njema; Mungu Akatenga nuru na giza. Mungu akaiita nuru Mchana, na giza Akaliita Usiku. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku moja."

**NB; Mungu Alifanya kazi toka siku ya kwanza ya Juma ambayo ni Jumapili. Siku ya kwanza Mungu aliumba nuru, na Akatenga nuru na giza. Mungu Akapumzika siku ya saba ambayo ni Sabato kwetu ni Jumamosi. Kwa hiyo Jumapili ni siku ya kazi na sio siku ya ibada.**

**Marko 16:9-12**

"Naye Alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, Alimtokea kwanza Mariamu Magdalene, ambaye kwamba Alimtoa pepo saba. Huyo akashika njia akawapasha habari wale waliokuwa pamoja naye, nao wakali wanaomboleza na kulia. Walakini hao waliposikia kama yu hai, naye Amemwona, hawakusadiki. Baada ya hayo Akawatokea watu wawili miongoni mwao, ana sura nyingine; nao walikuwa wakishika njia kwenda shamba.

**NB; Yesu Alipofufuka siku ya kwanza ya Juma ambayo ni Jumapili aliwatokea baadhi ya Wanafunzi Wake waliokuwa wakienda shamba. Kama ingekuwa Jumapili ni siku ya ibada Wanafunzi wa Yesu wasingeenda shamba.**

**Luka 23:54-56**

"Na siku ile ilikuwa siku ya Maandalio, na Sabato ikaanza kuingia. Na wale wanawake waliokuja Naye toka Galilaya walifuata, wakaliona kaburi, na jinsi mwili Wake ulivyowekwa. Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. Na siku ya Sabato walistarehe kama ilivyoamriwa.

**Luka 24:1**

"Hata siku ya kwanza ya Juma (Jumapili), ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini, wakiyaleta manukato waliyoweka tayari.

**NB; Akina mama (ambao walikuwa Wanafunzi wa Yesu) walipumzika siku ya saba (Sabato) ambayo ni Jumamosi, na Jumapili walifanya kazi ya kwenda kumpaka Yesu manukato lakini wakakuta amefufuka. Kwa hiyo Jumapili ni siku ya kazi na siyo siku ya ibada kulingana na Maandiko Matakatifu.**

**3. Yesu Alifufuka siku gani ya Juma?**

**Luka 24:1-3, 6**

"Hata siku ya kwanza ya Juma (Jumapili), ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini, wakiyaleta manukato waliyoweka tayari. Wakalikuta lile jiwe limevingirishwa mbali na kaburi, Wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu. Hayupo hapa, amefufuka. Kumbukeni Alivyosema nanyi Alipokuwa Akaliko Galilaya,

**4. Baada ya kufufuka Aliagiza watu waabudu siku ya Jumapili?**

**Mathayo 5:17-19**

"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua Torati au Manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, Basi mtu ye yote atakayevunja Amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni.

**5. Ni vigumu kiasi gani kubadilisha Amri za Mungu ikiwemo siku ya kuabudu?**
**Luka 16:17**
"Lakini ni vyepesi zaidi mbingu na nchi vitoweke, kuliko itanguke nukta moja ya Torati.
**NB; Yesu Alifufuka siku ya kwanza ya Juma yaani Jumapili, lakini hakufanya badiliko lolote la siku ya kuabudu toka siku ya saba (Sabato/ Jumamosi) kwenda Jumapili (siku ya kwanza ya Juma). Katika siku zote arobaini alizoisha hapa dunia baada ya kufufuka Kwake hakuna hata sehemu moja Alipoidhinisha badiliko la siku ya kuabudu. Jambo hili lilifanywa na wanadamu.**

**6. Imetupasa kumtii nani kati ya Mungu na wanadamu?**
**Matendo 5:29**
"Petro na Mitume wakajibu, wakisema, Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu."
**NB; Mpendwa ikiwa Mungu Ameagiza watu wamwabudu katika siku maalum alioiweka, na Mitume wanatushauri kumtii Mungu kuliko wanadamu, nakushauri umtii Mungu na kuanza kutunza Sabato ya Bwana.**

**7. Yesu alipokuwa duniani Aliabudu siku ya Jumapili?**
**Luka 4:16**
"Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya Sabato Akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi Yake, Akasimama ili asome.
**NB; Yesu alipokuwa duniani Hakuabudu siku ya Jumapili (siku ya kwanza ya Juma) bali siku ya Jumamosi (siku ya saba) ambayo ni Sabato ya Kweli.**

**8. Je? Jumapili ni siku ya Bwana?**
**Ufunuo 1:10**
"Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana; nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu"
**Marko 2:27, 28**
"Akawaambia, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya Sabato. Basi Mwana wa Adamu Ndiye Bwana wa Sabato pia."
**Kutoka 20:10**
"Lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako."
**Isaya 58:13**
"Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu Wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku Takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe;

**NB; Jumapili sio siku ya Bwana. Siku ya Bwana ni Sabato ambayo ni Jumamosi. Kwa kuwa Yesu Anasema Yeye ni Bwana wa Sabato (siku ya saba)**

**9. Mitume waliabudu siku gani? Jumamosi au Jumapili?**
**Matendo 18:4**
"Akatoa hoja zake katika sinagogi kila Sabato, akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani.
**Matendo 17:2**
"Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi Yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa Maneno ya Maandiko Sabato tatu,

**10. Wakristo wa kwanza waliabudu siku gani wakiwa pamoja na Mitume?**
**Matendo 16:13**
"Hata siku ya sabato tukatoka nje ya lango, tukaenda kando ya mto, ambapo tukadhani ya kuwa pana mahali pa kusali; tukaketi, tukasema na wanawake waliokutana pale."

**11. Miaka mingi baada ya msalaba Paulo anasema nini juu ya ibada ya siku ya saba ya Juma yaani Jumamosi?**
**Waebrania 4:9-11**
"Basi, imesalia raha ya Sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha Yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu Alivyostarehe katika kazi Zake. Basi, na tufanye bidi kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi."
**NB; Miaka mingi baada ya msalaba Neno la Mungu linasisitiza ibada ya siku ya saba ya Juma (Jumamosi) na sio siku ya kwanza ya Juma) Jumapili. Mtume Paulo anasisitiza watu wafanye bidii kuingia raha ya Sabato.**

**12. Kwa kuwa watu wengi wanaabudu siku ya Jumapili badala ya Sabato, Je, jambo hilo linaifanya Jumapili iwe siku halali ya kuabudu?**
**Isaya 8:20**
"Na waende kwa Sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno Hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi.
**Mwanzo 7:13**
"Siku ile ile Nuhu akaingia katika safina, yeye, na Shemu na Hamu na Yafethi, wana wa Nuhu, na mkewe Nuhu, na wake watatu wa wanawe pamoja naye;
**Mwanzo 7:21**
"Wakafa wote wenye mwili waendao juu ya nchi, na ndege, na wanyama wa kufugwa, na kila mnyama wa mwitu, na kila kitambaacho chenye kutambaa juu ya nchi, na kila mwanadamu;
**Mathayo 22:14**
"Kwa maana waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache."

**13. Je? Ni wengi wanaoweza kuiona njia ya Kweli (siku ya kuabudu iliyoagizwa na Mungu)?**
**Mathayo 7:13, 14**
"Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache."

**14. Katika nchi mpya wanadamu wataabudu siku gani? Jumapili au Jumamosi?**
**Isaya 66:22,23**
"Kama vile mbingu mpya na nchi mpya, Nitakazofanya, zitakavyokaa mbele Zangu, Asema Bwana, ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa. Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya, na Sabato hata Sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele Zangu, Asema Bwana.
**NB; Katika nchi mpya waliokombolewa wataabudu siku ya Sabato na sio siku ya kwanza ya Juma.**

**15. Ili kumrudia Mungu mtu Anatakiwa kufanya nini?**
**Isaya 55:6, 7**
"Mtafuteni Bwana, maadamu Anapatikana, Mwiteni, maadamu Yu karibu; Mtu mbaya na aache njia Yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye Atamsamehe kabisa.
**NB; Huu ni wakati wa kumgeukia Mungu na kuanza kutunza Sabato na kufanya ibada siku ambayo Mungu aliagiza yaani siku ya saba ambayo ni Jumamosi.**

**16. Mungu anaahidi nini?**
**Isaya 1:18-20**
"Haya, njoni, tusemezane, Asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu. Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi; bali kama mkikataa na kuasi mtaangamizwa kwa upanga; maana kinywa cha Bwana kimenena Haya."

**17. Ushauri gani Biblia inatupatia kupitia Mtume Petro?**
**1 Petro 2:21**
"Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo Naye Aliteswa kwa ajili yenu, Akawaachia kielelezo, mfuate nyayo Zake.

**18. Biblia inatoa wito gani kwako leo?**
**Warumi 14:12**
"Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu.
**Waebrania 4:9-11**
"Basi, imesalia raha ya Sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu

Alivyostarehe katika kazi Zake. Basi, na tufanye bidi kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi."

**NB; Tunaishi katika wakati wa mwisho ambapo kila mtu anapaswa kufanya maamuzi binafsi ya kumfuata Mungu wake. Ni vema kumchagua Yesu Kristo na Maneno Yake.**

**8)DALILI ZA KUJA KWA YESU MARA YA PILI**

**Kwa kuwa hatujui siku wala saa Bwana Yesu alitupatia nini?**

**a) Mathayo 24:3**

"Hata alipokuwa ameketi katika mlima wa Mizeituni, wanafunzi Wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja Kwako, na ya mwisho wa dunia?

**b) Marko 13:28, 29**

"Kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake liishapo kuwa laini, na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno ni karibu; nanyi kadhalika, myaonapo mambo hayo yanaanza, tambueni ya kuwa Bwana Yu karibu milangoni.

**NB; Ijapokuwa Bwana Yesu hakutupatia tarehe ya kurudi Kwake, Ametuachia dalili nyingi ambazo tukizichunguza kwa makini tutajua Dhahiri kuwa kuja Kwake kumekaribia. Tunaweza kuziweka dalili katika makundi kadhaa yafuatayo. Dalili za kiroho miongoni mwa wanadamu.**

**a) Ubinafsi kuzidi miongoni mwa wanadamu.**

**2 Timotheo 3:1-5**

"Lakini ufahamu Neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu Zake; hao nao ujiepushe nao"

**b) Kukataa mafundisho ya Kweli.**

**2 Timotheo 4:3,4**

"Maana utakuja wakati watakapoyakataa Mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe
watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo"

**c) Kubadilishwa kwa Amri za Mungu**

**Isaya 24:5**

"Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi Sheria, wameibadili Amri, wamelivunja Agano la milele"

**d) Kujitokeza kwa makanisa mengi na viongozi wanatumia unabii na miujiza kupoteza watu.**

**Marko 13:22,23**

“Kwa maana wataondoka makristo wa uongo, na manabii wa uongo, watatoa ishara na maajabu, wapate kuwadanganya, kama yamkini, hata hao wateule, Bali ninyi jihadharini; nimekwisha kuwaonya yote mbele.

**Dalili za kiafya katika dunia**
**a) Magonjwa yatakuwa mengi**
**Luka 21:11**
“Kutakuwa na matetemeko makubwa ya nchi; na njaa na ***tauni mahali mahali***; na mambo ya kutisha na ishara kuu kutoka mbinguni.

**b) Watu wengi watakufa**
**NB; Corona au Uviko19, kansa/saratani, kisukari, ukimwi, magonjwa ya moyo, UTI, ebola na magonjwa yasiyojulikana na yasiyo na tiba. Dalili toka angani**

**c) Jua, mwezi na Nyota**
**Yoeli 2:30**
“Nami nitaonyesha mambo ya ajabu katika mbingu na katika dunia, damu, na moto, na minara ya moshi. Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja hiyo siku ya Bwana iliyo kuu na itishayo.
**Mathayo 24:29**
“Lakini mara, baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota Zitaanguka mbinguni, na nguvu za mbinguni zitatikisika;
**NB; Usiku wa Novemba 12, 1833 nyota zilianguka toka mbinguni.**
**Ufunuo 6:12**
“Nami nikaona, alipoifungua muhuri ya sita, palikuwa na tetemeko kuu la nchi; jua likawa jeusi kama gunia la singa, mwezi wote ukawa kama damu,
**NB; Tetemeko hili ni lile la Lisbon la mwaka 1755 mwezi November tarehe 1. Walikufa watu 30, 000**

**Dalili za kimazingira zitakuwaje?**
**i) Njaa**
**Mathayo 24:7**
“Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali”
**NB; Kila siku watu 25,000 wanakufa kwa njaa, watoto wakiwa Zaidi ya elfe 10.**

**ii) Matetemeko**
**Mathayo 24:7**
“Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali.
**NB; Watu 9624 wakufa kwa matetemeko kati ya 2000 hadi 2015**

**Dal**

**ili za kisiasa**
**a) Vita baina ya mataifa**
**Luka 21:10**
"Aliwaambia, Taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme;
**b) Wakuu wa dunia watakosa la kufanya.**
**Isaya 24:4**
"Dunia inaomboleza, inazimia; ulimwengu unadhoofika, unazimia; watu wakuu wa dunia wanadhoofika"
**c) Kutengeneza silaha za vita, na kutaka kupigana.**
**Yoeli 3:9, 10**
"Tangazeni haya kati ya mataifa; takaseni vita; waamsheni mashujaa; watu wa vita na wakaribie; na wapande juu. Yafueni majembe yenu yawe panga, na miundu yenu iwe mikuki; aliye dhaifu na aseme, Mimi ni hodari"
**d) Dhiki hadi watu watakwenda kama vipofu,**
**Zephania 1:17**
"Nami nitawaletea wanadamu dhiki, hata watakwenda kama vipofu, kwa sababu wamemtenda Bwana dhambi; na damu yao itamwagwa kama mavumbi, na nyama yao kama mavi"

**Dalili za kielimu**
**a) Maarifa yataongezeka**
**Danieli 12:4**
"Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge Maneno Haya, ukakitie muhuri Kitabu, hata wakati wa mwisho; wengi wataenda mbio huko na huko, na ***maarifa yataongezeka"***
**b) Watu wakwenda huko na huko**
**Danieli 12:4**
"Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge Maneno Haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho; ***wengi wataenda mbio huko na huko***, na maarifa yataongezeka. **Dalili hizi zinatwambia nini?**
**Marko 13:29, 31**
"Nanyi kadhalika, myaonapo mambo hayo yanaanza, tambueni ya kuwa yu karibu milangoni. ***Amin, Nawaambieni, Kizazi hiki hakitapita, hata Hayo yote yatimie. Mbingu na nchi zitapita; lakini Maneno Yangu hayatapita kamwe"***
**Ufunuo 3:20**
"Tazama, Nasimama mlangoni, Nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, Nitaingia kwake, Nami Nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami. Yeye ashindaye, Nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi, kama Mimi Nilivyoshinda Nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi. ***Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa"***
**NB; Yesu alitoa unabii kabla ya kwenda mbinguni. Tunaona sehemu kubwa ya unabii Wake umetimilika. Mataifa yamekuwa yakiunda silaha zenye uwezo wa maangamizi makubwa sana. Dunia inapitia kipindi kigumu cha vita kubwa kubwa zinazochukua maisha ya watu wengi sana. Wakimbizi wametapakaa kila upande. Uhaba wa chakula ambao**

**husababisha vifo na kukosa lishe bora. Mlipuko wa magonjwa makubwa yanayogharimu serikali za dunia pesa nyingi sana. Amani imetoweka miongoni mwa wakaaji wa dunia inayosababishwa na migogoro isiyokuwa na majibu.**
**Kwa hakika ni dhahiri kuwa Bwana Yesu yu mlangoni.**

## 9)KUJA KWA YESU MARA YA PILI

**Kuja Kwa Yesu Kristo**
**1. Kabla ya kuondoka Yesu Aliahidi nini?**
**Yohana 14:2, 3**
"Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi; kama sivyo, Ningaliwaambia; maana Naenda kuwaandalia mahali" Basi Mimi Nikienda na kuwaandalia mahali, Nitakuja tena Niwakaribishe Kwangu; ili nilipo Mimi, nanyi mwepo"

**2. Tunaweza kuwa na uhakika kuwa Yesu atarudi tena?**
**Hesabu 23:19**
"Mungu si mtu, Aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo Amesema, hatalitenda? Iwapo Amenena, hatalifikiliza?"
**NB; Ni hakika kuwa, Yesu atarudi tena. Mungu hawezi kusema jambo na asilitimize.**

**3. Alienda kufanya nini?**
**Yohana 14:2**
"Maana Naenda kuwaandalia mahali"

**4. Atakuja tena kufanya nini?**
**Yohana 14:3**
"Basi Mimi Nikienda na kuwaandalia mahali, Nitakuja tena Niwakaribishe Kwangu; ili Nilipo Mimi, nanyi mwepo"

**5. Je? Atakuja kwa siri?**
**Mathayo 24:27**
"Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu"
**Ufunuo 1:7**
"Tazama, Yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili Yake. Naam. Amina" ·
**Matendo 1:11**
"Wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu Aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, Atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda Zake mbinguni"
**NB; Yesu hatakuja kwa siri kama wengine wanavyodhani. Siku atakapokuja watu wote walioko duniani watamwona. Kuja Kwake itakuwa jambo dhahiri kabisa.**

**6. Je? Kuna mtu anayejua siku Yesu atakuja mara ya pili?**

**Mathayo 24:36**
“Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata Malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke Yake” Ikiwa hatujui siku ya kuja Kwake,

**7. Je? Ametupatia dalili zozote zitakazo tusaidia kujua kuwa Anakaribia kuja?**
**Marko 13:28, 29**
“Kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake liishapo kuwa laini, na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno ni karibu, nanyi kadhalika, myaonapo mambo hayo yanaanza, tambueni ya kuwa Yu karibu milangoni”
**NB; Dalili nyingi za kuja kwa Yesu mara ya pili zimeandikwa katika injili ya Mathayo sura ya 24**.

**8. Kama hatujui siku isipokuwa dalili tu yatupasa kufanya nini?**
**Mathayo 25:13**
“Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa”

**9. Baadhi ya maandalizi ya kumpokea Yesu ajapo mara ya pili ni nini?**
**Kusoma biblia Yohana 17:3**
“Uzima wa milele ndio huu, Wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo Uliyemtuma”· Kuzungumza na Mungu kupitia Maandiko Matakatifu ·
**Kwenda mbele za Mungu na kuungama Isaya 1:18**
“Haya, njoni, tusemezane, Asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu”
**Kutubu Matendo 2:38**
“Petro akawaambia,Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu”

**10. Je? Atakapokuja hali ya watakatifu itakuwaje?**
**Isaya 25:9**
“Katika siku hiyo watasema, Tazama, Huyu Ndiye Mungu wetu, Ndiye Tuliyemngoja atusaidie; Huyu Ndiye Bwana Tuliyemngoja, Na tushangilie na kuufurahia wokovu Wake”. Walio makaburini watafufuliwa na walio hai kufumba na kufumbua watabadilishwa
**1WaKorintho 15:52**
“Kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika”

**11. Hali ya waovu itakuwaje? ·**
**Ufunuo 6:16**
“Wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso Wake Yeye Aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo”

**12. Hali ya viongozi wadini na Wakristo ambao hawakushika na kufundisha Amri za Mungu itakuwaje?**

**Mathayo 7:22**

"Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina Lako, na kwa jina Lako kutoa pepo, na kwa jina Lako kufanya miujiza mingi?

**Mathayo 7:23**

"Hapo Nitawaambia: Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni mbele Yangu, enyi watenda maovu"

**13. Hali ya dunia itakuwaje wakati wa kuja kwa Yesu mara ya pili?**

**Ufunuo 16:20**

"Kila kisiwa kikakimbia, wala milima haikuonekana tena"

**14. Hali ya matajiri wa dunia na wenye mali wasio mcha Bwana itakuwaje?**

**Ufunuo 6:15**

"Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba yamilima"

**15. Je? Fedha au dhahabu zitaweza kumsaidia mtu siku hiyo?**

**Zephania 1:18**

"Fedha yao wala dhahabu yao havitaweza kuwaokoa katika siku ile ya ghadhabu ya Bwana; bali nchi yote pia itateketezwa kwa moto wa wivu Wake; maana atawakomesha watu wote wakaao katika nchi hii, naam, ukomo wa kutisha"

**NB; Siku hiyo hakutakuwa na mwokozi, mtu hawezi kumsaidia mwenzake. Baba hawezi kumsaidia mtoto wake wala Mchungaji hata kuwa na msaada siku hiyo. Hata utajiri hautakuwa na nafasi katika kumsaidia mtu yeyote. Ni vema kila mtu afanye maamuzi yake mwenyewe binafsi.**

**16. Neno la Mungu linashauri nini? ·**

**Isaya 55:6, 7, (Tumtafute Mungu)**

"Mtafuteni Bwana, maadamu Anapatikana, Mwiteni, maadamu yu karibu; Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye Atamsamehe kabisa"

**Muhubiri 12:13 (Tumche Mungu na tuzishike Amri Zake)**

"Hii ndiyo jumla ya Maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike Amri Zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu" ·

**Matendo 3:19 (Mpokee Yesu kama Bwana Mwokozi wako sasa)**

"Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako Kwake Bwana"

**17. Mtu binafsi anatakiwa kufanya nini?·**
**Wagalatia 6:5 (Ijulikane kuwa kila mtu atabeba mzigo wake)**
"Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe" ·
**Warumi 14:12 (Jua kuwa utatoa habari zako mwenyewe)**
"Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu"

**18. Yesu Anasema nini kwako siku hii ya leo? Yesu Anakwambia nini siku ya leo?**
**Ufunuo 3:20**
"Tazama, Nasimama mlangoni, Nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, Nitaingia kwake, Nami Nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami"
**NB; Baada ya kujifunza vizuri kabisa juu ya kuja kwa Yesu mara ya pili na jinsi ya kuwa tayari inafaa kuyatoa maisha yako kwa Bwana Yesu ili uwe salama katika siku hiyo. Kumbuka Yesu Anapiga hodi katika mlango wa moyo wako. Bwana akubariki unapoendelea kutafakari mambo haya. Kumbuka kila mtu atatoa habari zake mwenyewe na pia atabeba mzigo wake mwenyewe.**

**10)KUNENA KWA LUGHA**
**1. Je? Yesu Alisema watu watanena kwa lugha?**
**Marko 16:17**
"Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya"

**2. Kunena kwa lugha kupo Bibliani?**
**Matendo 2:4**
"Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka"
**Matendo 19:6**
"Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri"

**3. Wanafunzi wa Yesu walipojazwa na Roho Mtakatifu wakati wa pentekoste ilikuwaje?**
**Matendo 2:1-4**
"Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi
kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyika na, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka"

**4. Wakati huo Yerusalemi kulikuwa na watu wa kutoka wapi?**
**Matendo 2:5**
"Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu"

**5. Wasiokuwa wayahudi waliwasikia wanafunzi waliponena kwa lugha, kwa lugha zao za asili yaani kule walikotoka?**
**Matendo 2:6-8**
"Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia
wakisema kwa lugha yake mwenyewe. Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama, hawa wote wasemao si Wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?
**NB; Baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu, wanafunzi wa Yesu walinena kwa lugha ambayo ilieleweka na watu waliokuwa wameitembelea Yerusalemu toka mataifa mbalimbali tofauti na makanisa mengi leo ambayo yananena kwa lugha ambazo hazieleweki. Kipawa cha lugha kilikuwa muhimu sana kwa kanisa la mwanzo lililokuwa likijiandaa kupeleka injili ulimwenguni kote.**

**6. Baadhi ya makabila yaliokuwepo ni yepi?**
**Matendo 2:9-11**
"Warparthi na Wamedi na Waelami, nao wakaao Mesopotamia, Uyahudi na Kapadokia, Ponto na Asia, Frigia na Pamfilia, Misri na pande za Libia karibu na Kirene, na wageni watokao Rumi, Wayahudi na waongofu, Wakrete na Waarabu; tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu.

**7. Paulo anasema nini juu ya kunena kwa lugha na kuhutubu?**
**1 Wakorintho 14:5**
"Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha, lakini Zaidi sana mpate kuhutubu, maana yeye ahutubuye ni mkuu kuliko yeye anenaye kwa lugha, isipokuwa afasiri, ili kusudi kanisa lipate kujengwa"
**NB; Kunena kwa lugha bila kufasiri hakujengi kanisa, kwa kuwa maneno yanayonenwa hayaeleweki. Kwa jambo hili Biblia iko wazi kabisa.**

**8. Paulo anasema nini kwa neno lisilojulikana?**
**1 Wakorintho 14:8, 9**
"Kwa maana baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejifanya tayari kwa vita? Vivyo hivyo na ninyi, msipotoa kwa ulimi neno lililo dhahiri, neno lile linenwalo litajulikanaje? Maana mtakuwa mkinena hewani tu.

**9. Kwa uhalisia lugha ni kwaajili ya nani?**
**1 Wakorintho 14:22**
"Basi, hizi lugha ni ishara, si kwao waaminio, bali kwao wasioamini lakini kuhutubu si kwa ajili yao wasioamini, bali kwa ajili yao waaminio.

**10. Je, Ilifika mahala kunena kwa lugha kukaleta machafuko katika makanisa ya awali?**
**1 Wakorintho 14:33**
"Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani; vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu"
**NB; Inaonyesha kuwa ilifika mahali unenaji kwa lugha ulileta machafuko makanisani ndio maana tunaona Mtume Paulo anaweka utaratibu juu ya suala zima la kunena kwa lugha. Hata leo sehemu mbalimbali watu hunena kwa lugha na kisha watu huanguka chini, na kisha wanasimulia huyo ni Roho Mtakatifu. Mambo haya yote yanapaswa kuchukuliwa tahadhari kabla ya mtu kujiunga nayo.**

**11. Paulo anaagiza nini juu ya utaratibu wa kunena kwa lugha?**
**1 Wakorintho 14:27**
"Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, tena zamu kwa zamu, na mmoja na afasiri"

**12. Kama hakuna mtu wa kufasiri Mtume Paulo ameagiza nini?**
**1 Wakorintho 14:28**
"Lakini asipokuwapo mwenye kufasiri na anyamaze katika kanisa; aseme na nafsi yake tena na Mungu"

**13. Kwanini anaagiza wakae kimya kanisani kama hakuna mtu wa kutasfiri?**
**1 Wakorintho 14:23**
"Haya! Ikiwa kanisa lote limekusanyika pamoja, na wote wanene kwa lugha, kisha ikawa wameingia watu wajinga au wasioamini, je! Hawatasema ya kwamba mna wazimu?

**14. Kwanini, tunatakiwa kuzingatia utaratibu huu wa kunena kwa lugha?**
**1 Wakorintho 14:33**
"Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani; vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu"
**2 Timotheo 3:16, 17**
"Kila Andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa Mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema"

**15. Mtume Paulo anatoa ushauri gani kwa makanisa leo ambayo waumini wote wananena kwa lugha bila kuwa na mtu wa kufasiri?**
**1 Wakorintho 14:40**
"Lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu"

**16. Je? kunena kwa lugha ni ishara ya utakatifu na kwamba mtu ameokoka?**
**NB; Hakuna mahali popote katika Biblia tunaposoma kuwa Yohana Mbatizaji alinena kwa lugha ijapokuwa alifanya uamsho mkuu kwa Israeli**

**na kufanya maadalizi ya kuja kwa Masihi. Hata Bwana wetu Yesu tunaona anaagiza kuwa mitume watanena kwa lugha mpya lakini yeye hakunena kwa lugha.**

17. **Biblia inasema nini kwa wale wasioyachunguza Maandiko?**
**Mathayo 22:29**
"Yesu akajibu, Akawaambia, Mwapotea, kwa kuwa hamyajui Maandiko wala uweza wa Mungu"
**Yeremia 50:6**
"Watu Wangu wamekuwa kondoo waliopotea, wachungaji wao wamewapoteza; wamewapotosha milimani; wamekwenda toka mlima hata kilima, wamesahau mahali pao pa kupumzika"
**18. Je? Lipo tumaini kwa wale watakaoisikia sauti ya Bwana Yesu na kuitii?**
**Yohana 10:16**
"Na kondoo wengine Ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao Imenipasa kuwaleta; na sauti Yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja" **NB; Mpendwa umejionea wazi juu ya Maagizo ya Mungu katika kunena kwa lugha. Ni vizuri ukaisikia sauti ya Mungu na kufanya kama anavyotaka kwa neema Yake. Pata muda wa kuyasoma Maandiko na kusikiliza sauti ya Mungu na kufanya uamuzi binafsi. Kumbuka, kila mtu atatoa habari Zake mbele Zake Mungu yeye mwenyewe.**

**11)<u>MIUJIZA</u>**

**<u>Miujiza ya Siku za Mwisho</u>**
**1. Biblia inatwambia nini juu ya hatari za siku za mwisho?**
**2 Timotheo 3; 1**
"Lakini ufahamu Neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari"

**2. Je, ni kweli kwamba wengi watayafuata mafundisho ya Uongo?**
**1 Timotheo 4:1**
"Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani"

**3. Mungu alionyesha kuwa siku za mwisho kutakuwa na uamsho mkuu miongoni mwa watu Wake?**
**Yoeli 2;28-30**
"Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba Nitamimina Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono; tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile, Nitamimina Roho Yangu. Nami Nitaonyesha mambo ya ajabu katika mbingu na katika dunia, damu, na moto, na minara ya moshi".

**4. Je? shetani naye ataigiza na kuleta uamsho bandia?**
**Ufunuo 16:14**

“Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi”

**Mathayo 24:23-25**

“Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au Yuko kule msisadiki. Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.Tazama, Nimekwisha kuwaonya mbele”

**NB; Ataleta manabii wengi wa uongo makanisani, atajifanya Kristo, atashusha moto kutoka mbinguni na pia ataigiza kuja kwa Yesu mara ya pili. Lakini ataanza na uamsho bandia. Ataigiza kuja kwa Yesu mara ya pili.**

**5. Je? miujiza ni ishara ya kuwa pamoja na Mungu?**

**Mathayo 7; 21-23**

“Si kila mtu Aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye Mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni. Wengi Wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa Jina Lako, na kwa Jina Lako kutoa pepo, na kwa Jina Lako kufanya miujiza mingi?Ndipo Nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu.

**6. Je? ni Mungu pekee Ndie mwenye uwezo wa kufanya miujiza?**

**Kutoka 7; 11-12**

“Ndipo Farao naye akawaita wenye akili na wachawi; na hao waganga wa Misri wakafanya vivyo kwa uganga wao. Wakabwaga chini kila mtu fimbo yake, nazo zikawa nyoka; lakini fimbo ya Haruni ikazimeza fimbo zao”

**Matendo 8:9-11**

“Na mtu mmoja, jina lake Simoni, hapo kwanza alikuwa akifanya uchawi katika mji ule, akiwashangaza watu wa taifa la Wasamaria, akisema ya kuwa yeye ni mtu mkubwa. Wote wakamsikiliza tangu mdogo hata mkubwa, wakisema, Mtu huyu ni uweza wa Mungu, ule Mkuu. Wakamsikiliza, kwa maana amewashangaza muda mwingi kwa uchawi wake”

**7. Roho za mashetani nazo zinaweza kufanya miujiza mikuu?**

**Ufunuo 16; 13, 14**

“Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi”

**NB; Simoni alifanya miujiza na maajabu makubwa hata watu wakadhani ni uwezo wa Mungu, kumbe ilikuwa ni nguvu za uchawi. Hata leo wengi hufanya miujiza na kuwaombea watu na wakati mwingine maombi yakajibiwa. Lakini ifahamike wazi kuwa sio miujiza yote inatoka kwa Mungu.**

**8. Nini madhara ya miujiza ya Uongo na uamsho bandia kwa Wakristo?**
**Kutoka 7:13**
"Moyo wa Farao ukawa ni mgumu asiwasikize; kama Bwana Alivyonena"
**NB; Miujiza ya Uongo na uamsho bandia vina madhara mabaya ya kuwafanya wakristo wawe na mioyo migumu na wasisikie Neno la Kweli la Mungu kama Farao wa Misri.**

**9. Wapo watakaopotezwa na miujiza ya shetani?**
**Mathayo 24; 10,**
"Ndipo wengi watakapojikwaa, nao watasalitiana, na kuchukiana"
**Mathayo 24:24**
"Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule"

**10. Kinga ya kutopotezwa na miujiza hii ni nini?**
**Zaburi 119:105**
"Neno Lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu"
**Zaburi 119:10-12**
"Kwa moyo wangu wote Nimekutafuta, Usiniache nipotee mbali na Maagizo Yako. Moyoni mwangu nimeliweka Neno Lako, Nisije Nikakutenda dhambi. Ee Bwana, umehimidiwa, Unifundishe Amri Zako"
**Isaya 8:20**
"Na waende kwa Sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno Hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi"
**NB; Wakristo wengi leo wameweka matumaini yao kwa Wachungaji, kila Mchungaji atakachosema ndicho wanachofanya. Wasahau kuwa Wachungaji wengine ni watumishi wa Ibilisi. Wakristo wanaacha kujisomea Neno la Mungu na kutafakari kwa makini waone kama wako kwenye njia ya Kweli au la. Pia Wakristo hawana Biblia ambayo ndiyo taa ya Mkristo. Leo katika makanisa mengi watu wanaimba mapambio usiku kucha lakini hawasomi kwa umakini Biblia na kuitafakari kwa undani. Usalama wetu upo katika Maandiko tu! Wachungaji wengi leo wamekuwa wafanyabiashara, wanajitajirisha kutokakwa waumini wao. Imefika wakati sasa kila Mkristo amtafute Mungu kwa bidii katika kuyasoma Maandiko Matakatifu.**

**11. Mtu anaweza kufanya miujiza lakini akakataliwa na Mungu siku ya mwisho**
**Mathayo 7; 21-23**
"Si kila mtu Aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye Mapenzi ya Baba Yangu Aliye mbinguni. Wengi Wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa Jina Lako, na kwa Jina Lako kutoa pepo, na kwa Jina Lako kufanya miujiza mingi?Ndipo Nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu.
**NB; Kwanini Yesu atawakataa watu japokuwa walifanya miujiza? Ni kwa**

**sababu hawakufanya Mapenzi ya Mungu na Kwenda sawa sawa na vile Neno Lake linavyosema.**

**Je? Mapenzi ya Mungu ni yapi? 1 Yohana 5:3**
"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike Amri Zake; wala Amri Zake si nzito"
**Yohana 14:15**
"Mkinipenda, mtazishika Amri Zangu"

**12. Kwani waliofanya miujiza wanaweza kukataliwa?**
**Mathayo 7; 22, 23**
"Wengi Wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa Jina Lako, na kwa Jina Lako kutoa pepo, na kwa Jina Lako kufanya miujiza mingi? Ndipo Nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu.
**NB; Watumishi hawa waliofanya miujiza watakataliwa sababu, hawakumtii Mungu kwa kumshika Amri Zake. Mambo ambayo Mungu Ameagiza kwenye Biblia hawakuyafanya; kama vile kutunza Sabato ya Bwana, kuweka sanamu makanisani nk. Mtumishi yeyote anayefanya miujiza au hata kunena kwa Lugha kama hatii Amri za Mungu basi huyo sio mtumishi aliyetumwa na Mungu na inafaa kumwepuka. Na kama hutafanya hivyo na wewe utakataliwa na Yesu siku ya mwisho.**

**13. Je? iko namna ya kumpima mtu huyo?**
**Kumbu 13;1-5**
"Kukizuka katikati yako nabii, au mwotaji wa ndoto, akikutolea ishara au ajabu, ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia akisema, Na tuifuate miungu mingine usiyoijua, tuitumikie hiyo; wewe usiyasikize maneno ya nabii yule, au yule mwotaji wa ndoto, kwa kuwa Bwana, Mungu wenu, yuawajaribu, apate kujua kwamba mwampenda Bwana, Mungu wenu, kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote. Tembeeni kwa kumfuata Bwana, Mungu wenu; mcheni na kushika Maagizo Yake na kuisikia sauti Yake, nanyi mtumikieni na kushikamana Naye. Na yule nabii, au yule mwotaji wa ndoto, na auawe, kwa kuwa amesema yaliyopotoka juu ya Bwana, Mungu wenu, aliyewatoa katika nchi ya Misri, akakukomboa katika nyumba ya utumwa, apate yule mtu kukupotoa katika njia Aliyokuamuru Bwana, Mungu wako, uiendee. Ndivyo utakavyouondoa uovu utoke katikati yako.
**Isaya 8:20**
"Na waende kwa Sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi"

**14. Kwani watumishi wanaweza kufanya jambo hili ambalo si zuri na ni la kupotosha?**
**Ezekieli 34:9,10**
"Kwa sababu hiyo, enyi wachungaji, lisikieni Neno la Bwana; Bwana MUNGU Asema hivi; Tazama, Mimi ni juu ya wachungaji; Nami Nitawataka kondoo Zangu mikononi mwao, Nami Nitawaachisha hiyo kazi ya kuwalisha kondoo; nao wachungaji hawatajilisha wenyewe tena; Nami Nitawaokoa kondoo Zangu

vinywani mwao, wasiwe tena chakula chao.
**NB; Inaonyesha watumishi wengi leo ni wale wanaoangalia faida yao binafsi. Wanajipatia faida wao binafsi bila kujali kondoo za Mungu. Ni wajibu wa kila mtu kujisomea Neno la Mungu yeye binafsi aone Mungu Anasema nini?**

**15. Je? Mungu amekaa kimya juu ya haya mambo makuu yanayokuja?**
**Ufunuo 18; 4, 5**
"Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake.
**NB; Maelfu wataondoka katika makanisa ambayo hayafundishi Kweli ya Mungu na kujiunga na kanisa la Mungu, kutoka sehemu mbali mbali na kona zote za dunia. Kanisa la Kweli utalitambua kwa kuona linafundisha Amri kumi za Mungu na upendo wa wokovu wa Yesu Kristo Bwana wetu. Mungu na akujalie hekima unapoyatafakari Maneno haya kwa kina.**

## 12)KANISA LA MUNGU

**1. Je? Mungu ana kanisa Lake?**
**Isaya 2:2,3**
"Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na mataifa yote watauendea makundi makundi. Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani kwa Bwana, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, Naye atatufundisha njia Zake, nasi tutakwenda katika mapito Yake maana katika Sayuni itatoka Sheria, na Neno la Bwana katika Yerusalemu.
**Mathayo 16:18**
"Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa Langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda."
**NB; Mungu analo kanisa Lake. Katika zama hizi za mwisho ataliweka wazi ili watu walimfahamu na kujiunga nalo.**

**2. Je? Wapo watu katika makanisa mengine ambao wanataka waje kwenye kanisa Lake?**
**Yohana 10:16**
"Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti Yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja.
**Ufunuo 18:4**
"Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake."

**3. Utalitambuaje kanisa la Mungu?**
**Isaya 8:20**
"Na waende kwa Sharia na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno Hili, bila shaka kwa hao hapana
asubuhi."

**Luka 6:44**
"Kwa kuwa kila mti hutambulikana kwa matunda yake; maana, katika miiba hawachumi tini, wala katika michongoma hawachumi zabibu.
**NB; Kanisa la Mungu lazima lizingatie Mafundisho ya Biblia na kushika Amri za Mungu kama zinafundishwa na Neno la Mungu.**

**4. Je? Upo wito maalum ambao Mungu anautoa katika Biblia ambao anataka walimwengu wajiunge na kanisa Lake?**
**Ufunuo 18:4**
"Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake."

5. **Kwanini Mungu anataka watu wajiunge na kanisa Lake?**
**Isaya 9:16**
"Kwa maana wawaongozao watu hawa ndio wawakoseshao, na hao walioongozwa na watu hao wameangamia."
**Yeremia 50:6**
"Watu Wangu wamekuwa kondoo waliopotea, wachungaji wao wamewapoteza; wamewapotosha milimani; wamekwenda toka mlima hata kilima, wamesahau mahali pao pa kupumzika."
**NB; Mungu anaona yako mafundisho mengi potofu katika makanisa ya leo. Ukweli wa biblia haufundishwi isipokuwa mapokeo ya wanadamu.**

**6. Ziko njia ngapi za wakovu?**
**Mathayo 7:13,14**
"Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache."
**NB; Wengine husema haijalishi njia unayopita kilicho muhimu ni kufika tuu, lakini Yesu anasema njia ya kufikia Ukweli halisi ni moja tu, tena ni nyembamba na ni wachache wanaoiona njia hiyo.**

**7. Yesu Anayaambia nini makanisa ya zama hizi?**
**Yohana 14:15**
"Mkinipenda, mtazishika Amri Zangu."

**8. Hizo Amri ziko wapi?**
I. **Kutoka 20:1-2**
"Mungu akanena Maneno haya yote akasema, Mimi ni Bwana, Mungu wako, Niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila Mimi.
**II. Kutoka 20:4-6**
"Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa Mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu Mwenye wivu; Nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, Nami Nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na

kuzishika Amri Zangu."

**III. Kutoka 20; 7**

"Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako, maana Bwana Hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye Jina Lake bure."

**IV.Kutoka 20:8-11**

"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana Alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, Akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana Akaibarikia siku ya Sabato Akaitakasa."

**V. Kutoka 20:12**

"Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako."

**VI.Kutoka 20:13**

"Usiue"

**VII. Kutoka 20:14**

"Usizini"

**VIII. Kutoka 20:15**

"Usiibe"

**IX. Kutoka 20:16**

"Usimshuhudie jirani yako uongo."

**X. Kutoka 20:17**

"Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho
nacho jirani yako".

**9. Unaweza kuwa Mkristo wa Kweli wakati hautii Amri za Mungu?**

**1 Yohana 2:4**

"Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki Amri Zake, ni mwongo, wala Kweli haimo ndani yake."

**10. Kanisa la mwisho la masalio litakuwa na sifa gani? Tatizo la Wakristo wa leo ni lipi?**

**Ufunuo 14:12**

"Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao Amri za Mungu, na imani ya Yesu."

**11. Hivi kuhama kanisa au dhehebu ni dhambi?**

**Matendo 26:4,5**

"Kwa maana Wayahudi wote wanajua maisha yangu tangu ujana, yaliyokuwa tangu mwanzo katika taifa langu huko Yerusalemu, wakinijua sana tangu mwanzo, kama wakipenda kushuhudia, ya kwamba nalikuwa Farisayo kwa kuifuata madhehebu ya dini yetu iliyo sahihi kabisa."

**12. Je? Mtume Paulo alipokutana na Yesu alifanya nini?**
**Matendo 26:15-17**
“Nami nikasema, Wewe u nani, Bwana? Bwana akaniambia, Mimi ni Yesu, Ambaye wewe Unaniudhi.
Lakini inuka, usimame kwa miguu yako, maana Nimekutokea kwa sababu hii, Nikuweke wewe uwe
Mtumishi na shahidi wa Mambo Haya uliyoyaona, na wa Mambo ambayo katika Hayo Nitajidhihirisha
kwako; Nikikuokoa na watu wako, na watu wa Mataifa, ambao nakutuma kwao;

**13. Tatizo la Wakristo wa leo ni nini?**
**Mathayo 7:21**
“Si kila mtu Aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye Mapenzi ya Baba Yangu Aliye mbinguni.”
**Luka 6:46**
“Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi Nisemayo?

**14. Kanisa la Kweli la Mungu litakuwa linaabudu siku gani?**
**Luka 4:16-19**
“Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya Sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi Yake, Akasimama ili asome. Akapewa Chuo cha Nabii Isaya, Akakifungua Chuo, Akatafuta mahali palipoandikwa, Roho wa Bwana yu juu Yangu, Kwa maana Amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.
**Kutoka 20:8-11**
“Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana Alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, Akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana Akaibarikia siku ya Sabato Akaitakasa.
**Waebrania 4:9-11**
“Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu Alivyostarehe katika kazi Zake. Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo
wa kuasi.
**NB; Kanisa la Mungu alie hai litakuwa linaabudu siku ambayo hata Mwana Wake Yesu aliabudu (Sabato, ambayo ni Jumamosi). Na pia litaabudu siku ya Sabato ambayo imeagizwa na Mungu katika Amri kumi. Mtume Paulo katika barua yake kwa Waebrania anashauri watu waingie katika raha ya Sabato (Jumamosi)**

**15. Hatima ya kanisa la Mungu ni ipi?**
**Ufunuo 7:9**

“Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao;
**NB; Hatimaye kanisa la Mungu litapata ushindi na kuingia katika raha ya milele.**

**13)WAFU WAKO WAPI?**

**1. Mtu aliumbwaje?**
**Mwanzo 2:7**
“Bwana Mungu Akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, Akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.

**2. Mtu anapokufa inakuwaje?**
**Muhubiri 12:7**
“Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, Nayo roho kumrudia Mungu Aliyeitoa”

**3. Pumzi puani wakati mwingine inaitwa nini?**
**Ayubu 27:3**
“Kwa kuwa uhai wangu ukali mzima ndani yangu, na roho ya Mungu i katika pua yangu;

**4. Roho inaweza kufa kulingana na Maandiko Matakatifu?**
**Ezekieli 18:4**
“Tazama, roho zote ni mali Yangu; kama vile roho ya baba ni mali Yangu, ndivyo ilivyo roho ya mwana mali Yangu; roho ile itendayo dhambi itakufa”

**5. Jina jingine la kifo ni nini katika biblia?**
**Danieli 12:2.**
“Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele”

**6. Mtu akifa ana kwenda mbinguni au motoni?**
**1wathesalonike 4:15 -17**
“Kwa kuwa twawaambieni haya kwa Neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja Kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana Mwenyewe Atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya Malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele”
**Danieli 12:2**
Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele.
**NB; Mtu akifa awe mdhambi au mtakatifu anarudi mavumbini, akisubiria**

**siku ya ufufuko. Akiwa kaburini hajui Neno lolote. Hivyo ndivyo Biblia inavyosema**.

**7. Wema wakifa wanaenda wapi?**
**Yohana 5:28**
"Msistaajabie Maneno Hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti
Yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima"
**Matendo 2:29-34**
"Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo. Maana Daudi hakupanda mbinguni; bali yeye mwenyewe anasema, abaya kwa ufufuo wa hukumu"

**8. Watu wabaya wakifa wanaenda wapi? Je? Ni motoni moja kwa moja?**
**Yohana 5; 28,29**
Msistaajabie Maneno Hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima,na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu.

**9. Je? Inafaa kuyakubali na kuyaamini Mafundisho ya Biblia kama hili la wafu?**
**2 Timotheo 3:16**
"Kila Andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa Mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema"

**10. Mtu anajua lolote kifoni?**
**Zaburi 6; 5**
"Maana mautini hapana kumbukumbu lako; Katika kuzimu ni nani atakayekushukuru?
**Muhubiri 9:5 -10**
"kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lo lote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa" Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja; wala hawana sehemu tena katika jambo lo lote lililofanyika chini ya jua. Lolote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako; kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe.

**11.Kisa cha Sauli na Samweli kina maana gani?**
**1Samweli 28:14, 15**
"Naye akamwuliza, Ni mfano wa nini? Akajibu, Ni mzee anazuka; naye amefunikwa vazi. Basi Sauli akatambua ya kwamba ndiye Samweli mwenyewe, akainama uso wake mpaka nchi, akasujudia. Ndipo Samweli akamwambia Sauli, Mbona umenitaabisha mimi, hata kunipandisha juu? Sauli akajibu, Mimi nimetaabika sana; kwa kuwa hao Wafilisti wananifanyia vita, Naye Mungu ameniacha;

hanijibu tena, wala kwa Manabii, wala kwa ndoto; kwa hiyo nimekuita wewe, ili wewe unijulishe nifanyeje"

**NB; Wakati kisa hiki kinatokea Samweli alikuwa ameshakufa. Malaika wa shetani walimwigiza Samweli. Tunaweza kuliamini hili kwa kuwa Biblia inatuambia wazi kuwa aliyekufa hajui neno lolote.**

**12.Je? shetani anaweza kujigeuza akawa mailaika wa nuru, au akaigiza sauti na sura ya mtu aliye kufa?**

**2 Wakorintho 11:14, 15**

"Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa Watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao"

**NB; Katika siku hizi za mwisho ni lazima tuchukue tahadhari kwa maana madanganyo ya Shetani yameongezeka sana na amekuwa mtaalamu zaidi katika kuwa danganya watu kupitia miujiza.**

wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe.

**13.Kisa cha Sauli na Samweli kina maana gani?**

**1Samweli 28:14, 15**

"Naye akamwuliza, Ni mfano wa nini? Akajibu, Ni mzee anazuka; naye amefunikwa vazi. Basi Sauli akatambua ya kwamba ndiye Samweli mwenyewe, akainama uso wake mpaka nchi, akasujudia. Ndipo Samweli akamwambia Sauli, Mbona umenitaabisha mimi, hata kunipandisha juu? Sauli akajibu, Mimi nimetaabika sana; kwa kuwa hao Wafilisti wananifanyia vita, Naye Mungu Ameniacha; hanijibu tena, wala kwa Manabii, wala kwa ndoto; kwa hiyo nimekuita wewe, ili wewe unijulishe nifanyeje"

**NB; Wakati kisa hiki kinatokea Samweli alikuwa amesha kufa. Malaika wa shetani walimwigiza Samweli. Tunaweza kuliamini hili kwa kuwa Biblia inatwambia wazi kuwa aliyekufa hajui neno lolote.**

**14.Je? shetani anaweza kujigeuza akawa mailaika wa nuru, au akaigiza sauti na sura ya mtu aliye kufa?**

**2 Wakorintho 11:14, 15**

"Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa Watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao"

**NB; Katika siku hizi za mwisho ni lazima tuchukue tahadhari kwa maana madanganyo ya Shetani yameongezeka sana na amekuwa mtaalamu zaidi katika kuwadanganya watu kupitia miujiza. Tukeshe tukiomba, tujisalimishe kwa Mungu 100%, tukae ndani Yake Bwana. Tunaambiwa atadiriki kuwadanganya hata wale walio wateule.**

**15. Je? Wapo wanaoweza kulikataa Fundisho hili?**

**2 Timotheo 4:3, 4**

"Maana utakuja wakati watakapoyakataa Mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa

wana masikio ya utafiti" nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.
NB; **Fundisho la Biblia juu watu waliokufa liko wazi kabisa, wao hawajui kitu chochote wala hawawezi kumsifu Mungu. Hata kama watafanyiwa mambo mabaya au mazuri hawajui kitu chochote. Mara nyingi shetani na mailaika zake wamekuwa wakiigiza maumbile au sauti za ndugu waliokufa ili kuwadanya watu. Umizimu yaani mambo kuhusu watu waliokufa kuwa bado hai, umeshamiri kwenye kila utamaduni. Mungu alimwumba mtu kutoka udongo na kumpulizia pumzi ya uhai.**
**Udongo + Pumzi ya Uhai (roho au nafsi)= Mtu hai. Roho haiwezi ikaishi mbali na mwili au kueleaelea angani. Huu ni udangayifu mkubwa, ulioanza Edeni, ukisema hakika hamtakufa. Kwahiyo wengi husema mtu akifa anaenda mbinguni moa kwa moja. Je, kwanini makaburi yafunguliwa na wafu watokee humo kama walikuwa mbinguni?**
**Lakini Biblia iko wazi kabisa kwa suala Hili. Hebu na tumtumikie Mungu wetu tukiwa hai. Hebu tuwajali wazazi wetu tukiwa hai, Kwani tukisha kufa tu, tutakuwa tumechelewa milele.**

## 14)ONYO LA MWISHO KWA DUNIA

**Pamoja na upendo mkubwa ambao Mungu ameuonyesha kwa ulimwengu, siku moja Atasema Maneno Haya mazito. Hapo ndio ukomo wa kila kitu utafika.**
**Ufunuo 22; 11**
"Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu;Mwenye uchafu na azaidi kuwa mchafu; na mwenye haki azidi kufanya haki; na Mtakatifu na azidi kuwa Mtakatifu"

**1. Je? Mungu Alishawahi kutoa kauli nzito katika ulimwengu wa kale?**
**a) Mwanzo 6:3**
"Bwana Akasema, Roho Yangu Haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini"
**b) Mwanzo 6:5-7**
"Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote" Bwana akaghairi kwa kuwa Amemfanya mwanadamu duniani, Akahuzunika Moyo. "Bwana Akasema, Nitamfutilia mbali mwanadamu Niliyemwumba usoni pa nchi; mwanadamu na mnyama, na kitambaacho na ndege wa angani; kwa maana naghairi ya kwamba Nimewafanya."

**2. Je? Utekelezaji wake ulikuwaje?**
**Mwanzo 7:20-23, 24**
"Maji yakapata nguvu, hata ikafunikwa milima kiasi cha mikono kumi na mitano. ***Wakafa wote wenye mwili*** waendao juu ya nchi, na ndege, na wanyama wa kufugwa, na kila mnyama wa mwitu, na kila kitambaacho chenye juu ya nchi, na kila mwanadamu; kila kitu chenye pumzi ya roho ya uhai puani mwake kikafa, kila kilichokuwako katika nchi kavu. ***Kila kilicho hai juu ya uso wa nchi***

***kikafutiliwa mbali tangu mwanadamu hata mnyama wa kufugwa***, na kitambaacho, na ndege wa angani; vilifutiliwa mbali katika nchi, ***akabaki Nuhu tu, na hao walio pamoja naye katika safina.***

**3. Je? Kuna wakati mwingine tena Mungu aliwaangamiza wanadamu?**
**i) Mwanzo 18:17, 18**
"Bwana Akanena, Je! Nimfiche Ibrahimu jambo nilifanyalo, akiwa Ibrahimu atakuwa taifa kuu, hodari, na katika yeye mataifa yote ya dunia watabarikiwa?
**ii) Mwanzo 18:20, 21**
"Bwana Akasema, Kwa kuwa kilio cha Sodoma na Gomora kimezidi, na dhambi zao zimeongezeka sana, basi, Nitashuka sasa Nione kama wanayotenda ni kiasi cha kilio kilichonijia; na kama sivyo, Nitajua.
**iii) Mwanzo 19:12, 13**
"Basi wale watu wakamwambia Lutu, Je! Unaye mtu hapa zaidi? Mkwe, wanao, na binti zako, na wowote ulio nao katika mji, uwatoe katika mahali hapa; maana tutapaharibu sisi mahali hapa, kwa kuwa kilio chake kimezidi mbele za Bwana; Naye Bwana Ametupeleka tupaharibu.
**Kilichofanyika Sodoma na Gomora**
**Mwanzo 19:23-25**
"Jua lilikuwa limechomoza juu ya nchi Lutu alipoingia Soari. Ndipo Bwana akanyesha juu ya Sodoma na juu
ya Gomora kiberiti na moto toka mbinguni kwa Bwana. Akaangusha miji hiyo na Bonde lote, na wote waliokaa katika miji hiyo, na yote yaliyomea katika nchi ile.

**4. Mungu anao wito anatoa katika ulimwengu wa leo pia.**
**i) Yesu ana kanisa moja tu**
**Yohana 10:14**
"Mimi Ndimi Mchungaji mwema; nao walio Wangu Nawajua; nao walio Wangu wanijua Mimi;
**Yohana 10:16**
"Na kondoo wengine Ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao Imenipasa kuwaleta; na sauti Yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na Mchungaji mmoja.
**ii) Mungu anatoa wito kwa watu Wake watoke katika Babeli ya kiroho ambayo inahusisha makanisa yote ambayo hayafundishi juu Amri za Mungu na upendo wa Yesu**
**5. Kitabu cha ufunuo kinasema nini juu ya sauti ya Mungu iliyosikika toka mbinguni?**
**Ufunuo 18:4, 5**
"Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake.

**6. Mambo yanayopelekea mwanadamu kukosa kumwani Yesu na kuishi kama Neno Lake lisemavyo kupotea milele ni yepi?**
**a) Kiburi na jeuri na kukataa kwa makusudi.**
**Kutoka 5:2**

“Farao akasema, Bwana ni nani, hata niisikilize sauti Yake, na kuwapa Israeli ruhusa waende zao? Mimi simjui Bwana, wala sitawapa Israeli ruhusa waende zao”

**b) Kuahirisha kupokea Ukweli wa Mungu.**

**Matendo 24:25**

“Na Paulo alipokuwa akitoa hoja zake katika habari ya haki, na kuwa na kiasi, na hukumu itakayokuja, Feliki akafanya hofu akajibu, Sasa enenda zako, nami nikipata nafasi nitakuita”

**c) Kuto mkiri na kumkana Yesu mbele za watu.**

**Mathayo 10;32**

“Basi, kila mtu atakaye Nikiri mbele ya watu, Nami Nitamkiri mbele ya Baba Yangu aliye mbinguni, bali mtu
yoyote atakaye Nikana, mbele ya watu , Nami Nitamkana mbele ya Baba Yangu Aliye mbinguni”

**d) Kuogopa kupoteza utukufu wa wanadaamu (watu watanionaje?)**

**Yohana 12:42,43**

“Walakini hata katika wakuu walikuwamo wengi waliomwamini; lakini kwa sababu ya Mafarisayo hawakumkiri, wasije wakatengwa na sinagogi. ***Kwa maana walipenda*** **utukufu** ***wa wanadamu kuliko utukufu wa Mungu.*** **Kwa wachungaji.**

**e) Kuona haya mbele za watu, na kuogopa kuwaambia kwel kwa vile wanaweza wasipate ajira**

**Luka 9;26**

“Kwa sababu kila atakayenionea haya Mimi na Maneno Yangu, Mwana wa Adamu Atamwonea haya mtu huyu, Atakapokuja katika utukufu Wake..”

**f) Kuogopa kutengwa kanisani**

**Yohana 12:42, 43**

“Walakini hata katika wakuu walikuwamo wengi waliomwamini; lakini kwa sababu ya Mafarisayo hawakumkiri, wasije wakatengwa na sinagogi. Kwa maana walipenda utukufu wa wanadamu kuliko utukufu wa Mungu”

**g) Kuhofia kukosa au kupoteza mambo ya dunia kama vile mali, urembo, kupoteza kazi**

**Mathayo 19:21,22**

“Yesu Akamwambia, Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo Unifuate. Yule kijana alipolisikia Neno Lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa
sababu alikuwa na mali nyingi.

**h) Kupenda mno baba, mama, mume, mke, mali , mtandao, elimu, mchungaji, ukoo na jamaa na marafiki**

**Mathayo 10:37, 38**

“Apendaye baba au mama kuliko Mimi, Hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko Mimi, Hanistahili. Wala mtu asiyechukua msalaba wake Akanifuata, Hanistahili”

**NB; Yesu Anabisha hodi ndani ya moyo wako, kwanini usingefungua mlango wa moyo wako na kumkaribisha.**

**7. Mungu Anakwambia nini Mkristo wa leo?**

**Ufunuo 3:19, 20**
"Wote Niwapendao Mimi Nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu. Tazama, Nasimama mlangoni, Nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, Nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami"

**8. Mungu ataendelea tu kunyoosha mikono Yake tu siku zote kwa wanadamu na kuwasihi wamgeukie Yeye?**

**Muhubiri 1:24-26**
"Kwa kuwa Nimeita, nanyi mkakataa; Nimeunyosha mkono Wangu, asiangalie mtu; Bali mmebatilisha Shauri Langu, Wala hamkutaka Maonyo Yangu; Mimi Nami Nitacheka siku ya msiba wenu, Nitadhihaki hofu yenu ifikapo"

**9. Wakati wa matukio ya kutisha na maangamizi ya siku za mwisho baada ya kufungwa kwa rehema, uhusiano wa Mungu na wanadamu utakuwaje?**

**Mithali 1:27-33**
"Hofu yenu ifikapo kama tufani, Na msiba wenu ufikapo kama kisulisuli, Dhiki na taabu zitakapowafikia. Ndipo watakaponiita, lakini sitaitika; Watanitafuta kwa bidii, wasinione. Hawakukubali Mashauri Yangu, Wakayadharau Maonyo Yangu yote. Kwa hiyo watakula matunda ya njia yao, Watashiba mashauri yao wenyewe. Maana kurudi nyuma kwao wajinga kutawaua, Na kufanikiwa kwao wapumbavu
kutawaangamiza. Bali kila anisikilizaye atakaa salama, Naye atatulia bila kuogopa mabaya"

**10. Neno la Mungu linakupatia ushauri gani?**

**Isaya 55:6, 7**
"Mtafuteni Bwana, maadamu Anapatikana, Mwiteni, maadamu Yu karibu; Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye Atamsamehe kabisa.

**11. Kumbuka kuwa moto haukuandaliwa kwaajili yako. Huo ni wa shetani na malaika zake, si wa mwanadamu, ni kama kuhudhuria karamu ambayo haukualikwa (gatecrash). Mwanadamu alianguka kwa kudanganywa, na Mungu akamtuma Mwanawe, malaika walipoanguka mbinguni, mkombozi hakufa kwaajili yao, ila nao walipewa muda wa toba.**

**Mathayo 25:41**
"Kisha Atawaambia na wale walioko mkono Wake wa kushoto, Ondokeni Kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, **aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake"**

**12. Yesu Anasema nini kwako na kwangu?**

**Ufunuo 3:20-22**
"Tazama, Nasimama mlangoni, Nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, Nitaingia kwake, Nami Nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami. Yeye ashindaye, Nitampa kuketi pamoja Nkatika kiti Changu cha enzi, kama Mimi Nilivyoshinda Nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi. Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho Ayaambia

makanisa.
**NB; Mpokee Yesu awe Bwana na mwokozi wako leo, utasalimika na kuingia katika ufalme Wake wa milele na milele.**

## 15)HUKUMU

**Hukumu ya Mungu**
**1. Biblia inasema nini juu ya hukumu?**
**Matendo 17:31**
"Kwa maana Ameweka siku Atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule Aliyemchagua; Naye amewapa watu wote uthabiti wa Mambo Haya kwa kumfufua katika wafu"

**2. Je? Ni wangapi watakao hukumiwa?**
**Warumi 14:10**
"Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu"
**2 Wakorintho 5:10**
"Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya."
**NB: Tukijua kuwa siku moja tutasimama mbele ya hukumu ya Mungu, yatupasa kuishi maisha matakatifu ili tusijekataliwa na Mwokozi wetu Yesu Kristo.**

**3. Je? Matendo mema bila kuwa na Yesu yatatusaidia?**
**Mathayo 7:22,23**
"Wengi Wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa Jina Lako, na kwa Jina Lako kutoa pepo, na kwa Jina Lako kufanya miujiza mingi? Ndipo Nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu"

**4. Nani alianzisha hiyo hukumu?**
**Danieli 7:9**
"Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja Aliye Mzee wa siku Ameketi; mavazi Yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa Chake kama sufu safi; kiti Chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu Zake moto uwakao"

**5. Ni wakina nani walisaidia katika kazi ya hukumu?**
**Danieli 7:10**
"Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele Zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi
wakasimama mbele Zake; hukumu ikawekwa, na Vitabu vikafunuliwa"
**NB; Malaika wa Mungu watashiriki katika kazi hii kubwa ya hukumu.**

**6. Je? Nini itatumika katika kuhukumu?**
**Yakobo 2:10, 11, 12**
"Maana mtu awaye yote atakayeishika Sheria yote, ila akajikwaa katika Neno moja, amekosa juu ya yote. Kwa maana Yeye Aliyesema, Usizini, pia Alisema, Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa
mvunja Sheria. Semeni ninyi, na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa Sheria ya uhuru"
**NB: Amri kumi ndio zitakazotumika katika mahakama hii ya mbinguni. Wale wote walio shindwa na kukataa kuzitii Amri kumi za Mungu, siku hiyo zitawageuka. Kwani Yesu hatakuwa upande wao. Maana Yeye Mwenyewe Alishika Amri za Mungu.**
**Yohana 15:10**
"Mkizishika Amri Zangu, mtakaa katika pendo Langu; kama vile Mimi Nilivyozishika Amri za Baba Yangu na kukaa katika pendo Lake"

**7. Je? Tunaye mtetezi katika mahakama hii ya mbinguni?**
**1 Yohana 2:1**
"Watoto Wangu wadogo, Nawaandikia Haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki"
**NB: Ni wale tu wanao mchagua na kumkiri Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wao, Atawatetea siku hiyo kuu. Wale tu wanaojiita kwa Jina Lake na kutenda sawa sawa na vile Anavyoagiza, ndio watakao tetewa.**
**Mathayo 7:21**
"Si kila mtu Aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye Mapenzi ya Baba Yangu Aliye mbinguni"

**8. Je? Kuna Nabii aliyefunuliwa juu ya hukumu?**
**Danieli 7:10**
"Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele Zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi
wakasimama mbele Zake; hukumu ikawekwa, na Vitabu vikafunuliwa"
**Ufunuo 20:12**
"Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na Vitabu vikafunguliwa; na Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile Vitabu, sawasawa na matendo yao".
**Amosi 4:12**
"Basi nitakutenda hivi, Ee Israeli, na kwa sababu nitakutenda hivi, ujiweke tayari kuonana na Mungu
wako, Ee Israeli"

**9. Mambo gani yataletwa hukumuni?**
**Mhubiri 12:14**
"Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya"

**10. Mambo ya hukumu yatakuwa ya vikundi?**
**Warumu 14:12**
“Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu”
**NB: Matendo yetu yote tunayoyatenda yanatunzwa katika kumbukumbu za Mungu. Malaika wa Mungu wanaona kila tunalolitenda. Hata kama ni la siri namna gani kwani hatuwezi kumficha. Ni vizuri kuziungama dhambi zetu na kuziacha. Kwani tukifanya hivyo tutafanikiwa katika siku hiyo kuu. Inafaa tujichunguze kila siku na kuona kama tunaenda kama Mungu Anavyotuagiza au la.**

**11. Maisha ya washindi au watakaopita katika hukumu hiyo yatakuwaje?**
**Ufunuo 21: 3, 4**
“Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na
wanadamu, Naye Atafanya maskani Yake pamoja nao, nao watakuwa watu Wake. Naye Mungu Mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye Atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita”

**12. Mungu anawapa washindi ahadi gani?**
**Ufunuo 21:7**
“Yeye ashindaye atayarithi haya, Nami Nitakuwa Mungu wake, Naye atakuwa Mwanangu”

**13. Hali ya waovu waliokataa kutii Amri za Mungu itakuwaje baada ya hukumu hii kubwa?**
**Ufunuo 21:8,**
“Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili”

**14. Je? Maneno haya tunajifunza juu ya hukumu ni ya Kweli,**
**Je? Mungu anasema nini?**
**Ufunuo** 21:5
“Na Yeye Aketiye juu ya kile kiti cha enzi Akasema, Tazama, Nayafanya yote kuwa mapya. Akaniambia,
Andika ya kwamba Maneno Hayo ni amini na Kweli” Yesu Anasema nawe siku hii ya leo?
**Ufunuo 3:20**
“Tazama, Nasimama mlangoni, nNbisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, Nitaingia kwake, Nami Nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami”
**NB: Mungu huwa hafanyi jambo bila kutuarifu ilitujiandae. Huu ni wakati wetu maalum kwaajili ya kujiandaa na hukumu ya Mungu.**
**Amosi 4:12**

“Basi Nitakutenda hivi, Ee Israeli, na kwa sababu Nitakutenda hivi, ujiweke tayari kuonana na Mungu wako, Ee Israeli” Ametufunilia juu ya huku hii kubwa inayokuja. Amatuonyesha nini tufanye ili tuwe salama. Hata ametuonyesha wazi kuwa ataisha na washindi. Lakini pia ametuonyesha hali itakayowapata waovu. Inafaa tumchague Yesu sasa katika maisha haya.

**15. Baadhi ya maandalizi ya hukumu ni yepi?**
**Shika Amri za Mungu (Mhubiri 12; 13)**
“Hii ndiyo jumla ya Maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike Amri Zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu”
**Tunza Sabato (Waebrania 4:9,11)**
“Basi, imesalia raha ya Sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu Alivyostarehe katika kazi Zake. Basi, na tufanye bidi kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi”
**Kutubu na kumpokea Yesu na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu (Matendo 2:38)**
“Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu”
**Yesu kukaa ndani Yetu (Yohana 15:5**)
“Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya Neno lolote”

## 16)MWISHO WA DUNIA

**1. Biblia inasemaje juu ya mwisho wa dunia?**
**Zefania 1; 14-15**
“Hiyo siku ya Bwana iliyo kuu i karibu; I karibu, nayo inafanya haraka sana; Naam, sauti ya siku ya Bwana;
Shujaa hulia kwa uchungu mwingi huko! Siku ile ni siku ya ghadhabu, Siku ya fadhaa na dhiki, Siku ya uharibifu na ukiwa, Siku ya giza na utusitusi, Siku ya mawingu na giza kuu”

**2. Je? Yesu na Wanafunzi Wake walizungumzia juu ya mwisho wa dunia?**
**Mathayo 24:3**
“Hata alipokuwa ameketi katika mlima wa Mizeituni, Wanafunzi Wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja Kwako, na ya mwisho wa dunia?

**3. Nabii Isaya inasemaje juu ya matukio ya mwisho wa dunia?**
**Isaya 24;20.**
“Dunia inalewalewa kama mlevi, nayo inawayawaya kama machela; na mzigo wa dhambi zake utailemea;
nayo itaanguka, wala haitainuka tena”
**Isaya 24;1, 4**
“Tazama, Bwana Ameifanya dunia kuwa tupu, Aifanya ukiwa, aipindua, na kuwatawanya wakaao ndani yake” Dunia inaomboleza, inazimia; ulimwengu

unadhoofika, unazimia; watu wakuu wa dunia wanadhoofika”

**4. Mwisho wa dunia utaandamana na nini?**
**Ufunuo 16; 14-18**
“Mbingu zikaondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa, na kila mlima na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake. Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kilamtumwa, na mwungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso Wake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?

**5. Neno la Mungu linashauri nini?**
**Isaya 55; 6, 7**
“Mtafuteni Bwana, maadamu Anapatikana, Mwiteni, maadamu Yu karibu; Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye Atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye Atamsamehe kabisa”
**Amosi 4; 12**
“Basi nitakutenda hivi, Ee Israeli, na kwa sababu nitakutenda hivi, ujiweke tayari kuonana na Mungu wako, Ee Israeli”
**Isaya 45:22, 23**
“Niangalieni Mimi, mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia; maana Mimi ni Mungu; hapana mwingine. Kwa nafsi Yangu Nimeapa, Neno Hili limetoka kinywani Mwangu katika haki, wala halitarudi, ya kwamba mbele Zangu kilagoti litapigwa, kila ulimi utaapa”
**NB; Kila wakati Mungu amekuwa akitoa Maonyo kabla hajafanya maangamizi yoyote. Wakati wa Nuhu alitoa onyo na wito kwa ulimwengu wa kale. Na sasa pia anatoa onyo juu ya matukio makuu yatakayotokea kabla ya kufungwa kwa historia ya dunia yetu. Anatuonya juu ya maovu ya dunia na tumchague yeye ilituwe salama. Anatushauri tumwangalie Yeye ili tuokolewa. Leo hii, watu wameangalia zaidi viongozi wa dini na kuacha kufuata Neno la Mungu linavyosema. Uangamivu utakuwa dhahiri kama ulivyotokea katika ulimwengu wa kale.**

**6. Wanaoendelea kukaidi Neno la Mungu Biblia inasema nini juu yao?**
**Marko 7:6 -9**
“Akawaambia, Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, Watu hawa huniheshimu kwa midomo Ila mioyo yao iko mbali Nami; Nao Waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu, Ninyi mwaiacha Amri ya Mungu, na kuyashika mapokeo ya wanadamu. Akawaambia, Vema! Mwaikataa Amri ya Mungu mpate kuyashika mapokeo yenu”
**Ufunuo 21:8**
“Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili”

**NB: Mbali na mapigo saba ya mwisho, Mungu Anasema ibada yao itakuwa ni bure kwa kuwa wamebadilisha Amri za Mungu na Maagizo Yake. Kwa mfano, wanaabudu siku ya kwanza ya juma ambayo ni Jumapili, wanabatiza watoto wachanga wakati Biblia haiungi mkono kitendi hicho na pia wanatengeneza sanamu wanaweka makanisani na kuzibudi kinyume na Maagizo ya Mungu. Yohana anaweka kuwa sehemu yao ni katika ziwa la moto.**

**7. Biblia inasema nini kwa wale wanaondelea kudhihaki juu ya Maonyo na Maelekezo ya Mungu?**
**Mithali 1:24-31**
"Kwa kuwa Nimeita, nanyi mkakataa; Nimeunyosha mkono Wangu, asiangalie mtu; Bali mmebatilisha Shauri Langu, Wala hamkutaka maonyo Yangu; Mimi Nami Nitacheka siku ya msiba wenu, Nitadhihaki hofu yenu ifikapo; Hofu yenu ifikapo kama tufani, Na msiba wenu ufikapo kama kisulisuli, Dhiki na taabu zitakapowafikia. Ndipo watakaponiita, lakini sitaitika; Watanitafuta kwa bidii, wasinione. Kwa kuwa walichukia maarifa, Wala hawakuchagua kumcha Bwana. Hawakukubali Mashauri Yangu, Wakayadharau Maonyo Yangu yote. Kwa hiyo watakula matunda ya njia yao, Watashiba mashauri yao wenyewe"

**8. Baadhi ya maandalizi ya kuja kwa Yesu na mwisho wa dunia ni nini?**
**Shika Amri za Mungu (Mhubiri 12; 13)**
"Hii ndiyo jumla ya Maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike Amri Zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu"
**Tunza Sabato (Waebrania 4:9,11)**
"Basi, imesalia raha ya Sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha Yake amestarehe
mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu Alivyostarehe katika kazi Zake. Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi"
**Kutubu, kumpokea Yesu na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu (Matendo 2:38)**
"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"
**Yesu kukaa ndani Yetu (Yohana 15:5)**
"Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya Neno lo lote"

## 17)NENO LA MUNGU LIKO WAZI

**Kwanini watu wengi wanapotea wakati Neno la Mungu liko wazi?**
**1. Hawana Biblia yaani Neno la Mungu.**
**Zaburi 119:105**
"Neno Lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.
**Yohana 17:17**
"Uwatakase kwa ile Kweli; Neno Lako ndiyo Kweli.
**2. Hawajui Maandiko yaani Neno la Mungu.**

**Mathayo 22:29**
“Yesu akajibu, Akawaambia, Mwapotea, kwa kuwa hamyajui Maandiko wala uweza wa Mungu.

**3. Hawayachunguzi Maandiko na hutegemea kusomewa na viongozi wa dini.**
**Matendo 17:11**
“Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile Neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza Maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.
**NB; Watu wengi siku hizi hawana muda wa kusoma Neno la Mungu na kulitafakari. Hutumia muda mwingi kwenye mitandao ya kijamii na Kuangalia Runinga. Na wanapokuwa kanisani wanasomewa tu Mafungu ya Biblia bila wao wenyewe kusoma na kujua Mungu Anawaambia nini. Jambo hili limefanya wengi wapotee.**
**Isaya 28:13**
“Kwa sababu hiyo Neno la Bwana kwao litakuwa hivi, Amri juu ya Amri, Amri juu ya Amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo; ili waende na kuanguka nyuma, na kuvunjwa, na kunaswa, na kuchukuliwa.

**4. Manabii wa uongo wamekuwa wengi siku hizi na kazi yao kubwa ni kujipatia faida toka kwa waumini wao kwa njia yoyote hata kama ni ya uongo**
**Mathayo 24:24,25**
“Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule. Tazama, Nimekwisha kuwaonya mbele.

**5. Je? Biblia imetabiri juu waalimu wa uongo watakaopoteza watu pia?**
**2 Petro 2:1**
“Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana Aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia.
**NB: Mambo ya kutisha yanafanyika makanisani siku hizi. Kama wengi wangesoma Neno la Mungu wangeuona wazi udanganyifu wa shetani ambao uko wazi.**

**6. Waumini wengi wanapenda maneno laini na yadanganyayo.**
**Isaya 30:9-11**
“Kwa maana watu hawa ni watu waasi, watoto wasemao uongo, watoto wasiotaka kuisikia Sheria ya Bwana; wawaambiao waonaji, Msione; na Manabii, Msitoe unabii wa mambo ya haki, tuambieni maneno laini, hubirini maneno yadanganyayo; tokeni katika njia, geukeni mtoke katika mapito; mkomesheni Mtakatifu wa Israeli mbele yetu.

**NB: Wakristo wengi siku hizi wanapenda mambo rahisi, Ukweli unapowekwa wazi wanakasirika hata wengine wanaacha imani. Wanaona ukristo ni mgumu. Hawako tayari kuachana na vyakula au vinywaji ambavyo Neno la Mungu linakataza. Hawako tayari kujikana nafsi na kumfuata Yesu Kristo. Wanapenda dunia kuliko kumpenda Mungu.**

**7. Wachungaji wanaoaminiwa ndio wanawadanganya.**
**Isaya 9:16**
"Kwa maana wawaongozao watu hawa ndio wawakoseshao, na hao walioongozwa na watu hao wameangamia.
**Yeremia 50:6**
"Watu Wangu wamekuwa kondoo waliopotea, wachungaji wao wamewapoteza; wamewapotosha milimani: wamekwenda toka mlima hata kilima, wamesahau mahali pao pa kupumzika.

**8. Watu wengi wanapenda dunia kuliko kumpenda Mungu.**
**1 Yohana 2:15, 16**
"Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia.
**Mathayo 6:24**
"Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.

**9. Waumini wengi wamekuwa wakristo wa jina tu, kumpenda Mungu kuko mbali nao.**
**Luka 6:46**
"Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi Nisemayo?
**Mathayo 7:21-23**
"Si kila mtu Aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye Mapenzi ya Baba Yangu Aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa Jina Lako, na kwa Jina Lako kutoa pepo, na kwa Jina Lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu.

**10. Hawaioni njia nyembamba bali ile pana tu.**
**Mathayo 7:13,14**
"Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.
**Mathayo 16:24**
"Wakati huo Yesu Aliwaambia Wanafunzi Wake, Mtu ye yote akitaka Kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, Anifuate."
**NB; Kumfuata Mungu siyo jambo rahisi. Inahitaji maombi mengi na**

**kujikana nafsi kila siku. Wengi wanaishia kuchagua njia pana iendayo upotevuni na kuiacha nyembamba inayowaelekeza mbingu.**

**11. Wengi wanadhani misisimko ndiyo dini ya Kweli.**
**Yohana 4:24**
"Mungu ni Roho, nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na Kweli.
**1 Wafalme 18:26, 28**
"Wakamtwaa yule ng'ombe waliyepewa, wakamtengeza, wakaliitia jina la Baali tangu asubuhi hata adhuhuri, wakisema, Ee Baali, utusikie. Lakini hapakuwa na sauti, wala aliyejibu. Nao wakaruka-ruka juu ya madhabahu waliyoifanya. Wakapiga kelele, wakajikata-kata kwa visu na vyembe kama ilivyo desturi yao, hata damu ikawachuruzika.
**1 Yohana 4:1-3**
"Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani. Katika hili mwamjua Roho wa Mungu; kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu. Na hii ndiyo roho ya mpinga Kristo ambayo mmesikia kwamba yaja; na sasa imekwisha kuwako duniani.
**NB; Usiongozwe na misisimko bali ongozwa na Neno la Mungu. Pia yafaa kuzichunguza roho.**

**12. Wengi wanategemea miujiza badala ya Ukweli wa Neno la Mungu.**
**Mathayo 7:21-23**
"Si kila mtu Aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye Mapenzi ya Baba Yangu Aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa Jina Lako, na kwa Jina Lako kutoa pepo, na kwa Jina Lako kufanya miujiza mingi? Ndipo Nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu.

**13. Wanaamini watu zaidi kuliko Neno la Mungu.**
**Mathayo 10:37**
"Apendaye baba au mama kuliko Mimi, Hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko Mimi, Hanistahili.

**14. Wanaogopa kutengwa na kanisa.**
**Yohana 12:42,43**
"Walakini hata katika wakuu walikuwamo wengi waliomwamini; lakini kwa sababu ya Mafarisayo hawakumkiri, wasije wakatengwa na sinagogi. Kwa maana walipenda utukufu wa wanadamu kuliko utukufu wa Mungu.
**NB; Ikiwa umeamua kumfuata Mungu wa Kweli hata kama kanisa litakutenga hautapata madhara yoyote kwa sababu umefanya uamuzi ulio bora. Kumbuka mtume Paulo alipomwamini Yesu Kristo Aliachana na dini Yake ya kifarisayo na kumfuata Yesu hivyo basi hakuna laana yoyote itakayokupata kwa kumchagua Yesu. Cheo, mali, fahari ya dunia**

**visikuzuie kumfuata Bwana wako Aliyekufia msalabani.**

**15. Mtu anapaswa kufanya nini ili asipotezwe?**
**I. Kuwa na Biblia yako mwenyewe.**
**Zaburi 119:105**
"Neno Lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.
**Yohana 17:17**
"Uwatakase kwa ile Kweli; Neno Lako ndiyo Kweli.
**NB; Biblia ndio Kiongozi pekee kutuelekeza kwa Mungu. Ni Neno Lake lililovuviwa. Ni vizuri kuwa nayo maana Mungu Anajifunua kupitia Biblia. Mungu amepanga kututakasa kupitia Neno Lake.**

**II. Isome (ichunguze) Biblia yako kwa maombi na tafakari.**
**Matendo 17:11**
"Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea Lile Neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza Maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.
**Isaya 28:13**
"Kwa sababu hiyo Neno la Bwana kwao litakuwa hivi, Amri juu ya Amri, Amri juu ya Amri; Kanuni juu ya Kanuni, Kanuni juu ya Kanuni; huku kidogo na huku kidogo; ili waende na kuanguka nyuma, na kuvunjwa, na kunaswa, na kuchukuliwa
**NB: Isome Biblia kwa maombi mengi na kwakulinganisha mstari kwa mstari utaelewa kile Mungu anachotaka ufanye. Roho Wake atakuwa karibu nawe kukuelekeza na kukufanya uielewe vizuri.**

**III. Ishi kulingana na Neno la Mungu linavyosema.**
**Luka 6:46**
"Na kwa nini Mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi Nisemayo?
**Mathayo 7:21-23**
"Si kila mtu Aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye Mapenzi ya Baba Yangu Aliye mbinguni. Wengi Wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina Lako, na kwa jina Lako kutoa pepo, na kwa jina Lako kufanya miujiza mingi? Ndipo Nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu.
**NB: Wakristo wengi leo ni Wakristo jina tu, maana hawaishi kama Neno la Mungu linavyosema. Hawatunzi Sabato ya Bwana wala hawatii Amri za Mungu kwa neema ya Yesu Kristo. Dini ya misisimko imetawala pia**

**IV.Usiweke matumaini yako (imani) kwa wanadamu kuliko kumsikiliza Mungu. Biblia si kitabu cha kutupa habari tu, bali ni kitabu cha kubadilishwa. Ni sauti ya Mungu Mwenyewe, kama vile ambavyo angezungumza nawe uso kwa uso. Baada ya dhambi Mungu hakuzungumza na watu uso kwa uso, hivyo Mungu anazungumza nasi kupitia vitabu Vyake vitatu, navyo ni Asilia au nature, Biblia, na Kupitia**

**Patakatifu, ule mchoro, ni mafundisho ambayo Mungu ameweka kwenye picha ili kutufundisha, na kisha tuelewe kwa urahisi. Na hivyo tunapaswa kumpenda Yeye kwa moyo wetu wote na nguvu, na akili, na roho. Mathayo 10:37**

"Apendaye baba au mama kuliko Mimi, Hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko Mimi, Hanistahili.

**Yeremia 17:5**

"Bwana Asema hivi, Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, Amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake Na moyoni mwake amemwacha Bwana.

**Ezekieli 34:10**

"Bwana MUNGU Asema hivi; Tazama, Mimi ni juu ya wachungaji; Nami Nitawataka kondoo Zangu mikononi mwao, Nami Nitawaachisha hiyo kazi ya kuwalisha kondoo; nao wachungaji hawatajilisha wenyewe tena; Nami Nitawaokoa kondoo Zangu vinywani mwao, wasiwe tena chakula chao.

**NB; Wengi wameweka matumaini yao kwa wazazi, ndugu jamaa na marafiki na hata wachungaji. Lakini Neno la Mungu linatuonya kuwa tusiweke matumaini yetu kwa watu maana watu wana udhaifu mwingi. Wapo wachungaji wengi leo wanaojipatia faida binafsi toka kwa waumini wao. Wako tayari hatakutumia mbinu zisizofaa maadam tu wajipatie faida wao binafsi bila kujali washiriki wao.**

**Hii imesababisha manabii wa uongo wanaofanya miujiza bandia ili tu wajipatie pesa. Mpendwa mtafute Mungu wa Kweli hapo utakuwa salama. Bwana hatakawia, dalili zinaonyesha Yeye atarudi hivi karibuni. Nasi tungependa tumfuate Mwana-Kondoo kila tunapokwenda. Biblia inasema kwamba kwa Bwana siku moja ni miaka elfu moja kwetu, hivyo hata wakina Methuselah, au Adamu walioishi sana waliishi masaa kama 20 hivi, na sisi tukiishi miaka 70 tutakuwa tumeishi masaa 2 tu, Milele ni muda mrefu, na maisha yanakuwa bora tukiamua kuwa kule, maana hakika tutakuwa na furaha ya kweli, nami pia naamini Yale Bwana amesema Tuombeane.**


YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, "Njoo!" Kila mtu asikiaye hili, na aseme, "Njoo!" Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina

Grace Momadi-Masaka na Daniel Masaka,

---

***Kwa Maswali na Majibu:***
*Simu: +255 -755 -040766*
*Mbeya - Tanzania.*
*Barua pepe: kwelizabiblia@gmail.com*

---



Journeys of Abraham, Isaac and Jacob
ConformingToJesus.com
Journeys of Abraham
Journeys of Isaac
Journeys of Jacob
Main Roads
FERTILE CRESCENT
MESOPOTAMIA
PADDAN-ARAM
CHALDEA
Tigris
Euphrates
Mediterranean Sea
Ur
Babylon
Niniveh
Haran
Carchemish
Tadmor
Hobah
Damascus
Laish
Shechem
Bethel
Moriah
Hebron
Beersheba
Gerar
Kadesh
EDOM
PARAN
SHUR
EGYPT
GOSHEN


Invasion and Conquest of Canaan
Gathering of the Canaanite army
Canaanite army retreat
Hebrew army
Hebrew Central campaign
Hebrew Southern campaign
City attacked and burned
Site of battle
Great Sea
GESHER
GILEAD
CANAAN
PHILISTIA
Sea of Chinnereth
(Sea of Galilee)
Salt Sea
(Dead Sea)
Lake Huleh
Jordan
Tyre
Dan
Hazor
Madon (?)
Acco
Megiddo
Jezreel
Beth-shean
Shechem
Joppa
Bethel
Ai
Gibeon
Gilgal (?)
Jericho
Jerusalem
Azekah
Libnah
Lachish
Eglon
Hebron
Debir
The Historical Atlas of the Bible (2006) Cartographica Press


Physical Features of Palestine
Mediterranean Sea
I. Coastal Plain
II. Hill Country
III. Jordan Valley
IV. Trans-jordan Plateau
Scale of Miles
0 10 20 30 40
N
E
S
W
Sidon
Tyre
PHOENICIA
MT. LEBANON
Litani R.
MT. HERMON
Damascus
Dan
UPPER GALILEE
Lake Huleh
Hazor
BASHAN
Plain of Accho
LOWER GALILEE
Sea of Galilee
Yarmuk R.
Mt. Carmel
Kishon R.
Nazareth
Mt. Tabor
Dor
Megiddo
Jezreel
Mt. Gilboa
Caesarea
Plain of Sharon
SAMARIA
Mt. Ebal
Shechem
Mt. Gerizim
GILEAD
Jabbok R.
Jordan River
EPHRAIM
Joppa
I
II
III
IV
KINGS HIGHWAY
ARABIAN DESERT
Jericho
Jerusalem
Mt. of Olives
Bethlehem
Mt. Nebo
Plain of Philistia
Shephelah
JUDEA
Lachish
Hebron
Gaza
Dead Sea
Arnon R.
AMMON
WAY OF THE SEA
Beersheba
Wilderness of Judah
MOAB
WAY OF SEIR
River of Egypt
Zered R.
NEGEB
Arabah
EDOM
Kadesh-barnea
©2009 S. Scott Richardson Sr., Russellville AL


THE KINGDOMS OF
ISRAEL AND JUDAH
1 KINGS 12
PHOENICIA
Sidon
Tyre
Dan
Jeroboam built a sanctuary
Damascus
ARAM
Akko
Sea of Galilee
ISRAEL
Kamon
Megiddo
Political capital of Israel from Omri onward
Jordan River
Mediterranean Sea
Samaria
Shechem
Adam
Jeroboam built a sanctuary
Jaffa
Bethel
Ai
Rabbath-Ammon
Ashdod
Jericho
AMMON
Jerusalem
Ashkelon
Lachish
Gaza
Hebron
Dibon
Dead Sea
Debir
PHILISTIA
Beersheba
MOAB
JUDAH
Zoar
Tamar
EDOM
Kadesh Barnea
CONFORMINGTOJESUS.COM


PALESTINE IN THE TIME OF JESUS
By Mark Barry © 2011 Please do not republish without permission, but feel free to copy for personal use.
MEDITERRANEAN SEA
Damascus
SYRIA
Mt. Hermon
Caesarea Philippi
Sidon
Zarephath
Tyre
PHOENICIA
TRACHONITIS
Seleucia
Ptolemais
Korazin
Capernaum
Gennesaret
Bethsaida
Magdala
Naveh
Cana
Gergesa
Tiberias
Sea of Galilee
Sepphoris
Mt. Tabor
Dium
Nazareth
Abilene
GALILEE
Nain
Gadara
Caesarea
Scythopolis
DECAPOLIS
Pella
SAMARIA
Samaria
Gerasa
Shechem
Sychar
Mt. Gerizim
Jordan River
Antipatris
Gedora
Joppa
Arimathea
PEREA
Lydda
Ephraim
Philadelphia
Jamnia
Jericho
Emmaus
Mt. Olives
Jerusalem
Azotus
Bethany
Qumran
Bethlehem
Ashkelon
JUDEA
Machaerus
Hebron
Gaza
Dead Sea
En Gedi
IDUMEA
Masada
Raphia
Beersheba
Elusa
Zoar
NABATEA
Mampsis
N


MAP OF PAUL'S MISSIONARY JOURNEYS
Paul's first journey
Paul's second journey
Paul's third journey
Paul's voyage to Rome
City
One of the "Seven Churches"
ConformingToJesus.com
BLACK SEA
AEGEAN SEA
MEDITERRANEAN SEA
TYRRHENIAN SEA
ADRIATIC SEA
MACEDONIA
THRACE
BITHYNIA & PONTUS
GALATIA
CAPPADOCIA
CILICIA
COMMAGENE
SYRIA
NABATEA
JUDEA
EGYPT
CYRENAICA
ACHAIA
ASIA
MYSIA
PHRYGIA
PAMPHYLIA
LYCIA
ITALY
SICILY
MALTA
CRETE
CYPRUS
Syrtis Minor
Syrtis Major
Euphrates River
Orontes River
Jordan River
Nile River
Tiber River
DEAD SEA
Rome
Three Tavers
Appii Forum
Puteoli
Pompeii
Tarentum
Brundisium
Rhegium
Messina
Syracuse
Thessalonica
Berea
Amphipolis
Apollonia
Philippi
Neapolis
SAMOTHRACE
Troas
Assos
Mytilene
CHIOS
SAMOS
Ephesus
Smyrna
Pergamum
Thyatira
Sardis
Philadelphia
Laodicea
Miletus
Cnidus
COS
RHODES
Byzantium
Delphi
Corinth
Cenchreae
Athens
Olympia
Sparta
CYCLADES ISLANDS
Salmone
Lasea
Fair Havens
Phoenix
CLAUDA
Cyrene
Alexandria
Memphis
Patara
Myra
Attalia
Perga
Lystra
Derbe
Iconium
Antioch in Pisidia
Tarsus
Salamis
Paphos
Antioch
Seleucia Pieria
Damascus
Sidon
Tyre
Ptolemais
Caesarea Maritima
Antipatris
Jerusalem
Paul preaches the Gospel for 2 yrs under house arrest as he awaits for his appeal to Caesar
Ship lost in storm Paul swims safely to shore
Paul speaks at the Areopagus
Lydia & her household believe Paul & Silas beaten & thrown in jail Jailer and his household believe
Paul restores life to young Eutychus
Paul & Barnabas mistaken for gods Paul stoned
Timothy joins Paul & Silas
Proconsul Sergius Paulus converted
Jerusalem Conference c. 49-50 AD
Paul sent to Rome to appeal to Caesar
0 100 200 300 Miles
0 100 200 300 Kilometers

**Waandishi Grace Momadi-Masaka na Daniel Masaka**

Biblia ni kitabu kilichobadilisha maisha ya watu duniani kuliko kitabu kingine chochote kwa kuwa ni sauti ya MUNGU Mwenyewe iliyo na mamlaka ya mwisho duniani na mbinguni. Hakuna aliyesoma Kemia na kusema imemsaidia kuacha tabia ya uongo au dhambi. Neno la Mungu peke yake ndilo ambalo huleta tabia njema kwa watoto na watu wazima.

Walikuja kumwamini MUNGU kupitia unabii wa Danieli 2, wakiwa chini ya umri wa miaka 12. Unabii huu uliwaelezea kwamba Biblia inaendana na historia ya kweli ya mwanadamu iliyoanza Edeni na ambayo leo ipo kwenye mitaala ya shule na mitandao, nayo haizidi miaka 6000. Masihi katika Daniel 24:15 aliwahusia watu wasome unabiii huu. Asilimia 75 ya watoto wote humwamini Mwenyezi Mungu kama Muumbaji, Mdumishani na Mkombozi wao kabla ya kufika miaka 10! Na asilimia moja tu baada ya miaka 53! Lisome, Likariri, Litafakari, na Liishi NENO hili mchana na usiku. Nadharia zingine potofu kama uibukaji kwa kawaida huaminiwa na watu wazima zaidi, japo masimulizi yake ni ubunifu wa nchi za mbali zisizo na sokwe. Hii inatubidisha wazazi kuwalea watoto katika njia inayopasa nao wanapokuwa wazee hawataweza kuisahau, na siku moja watakuwa na Mwenyezi Mungu Mbinguni milele zote. Mbingu ni bure, tuombeane tusiikose kwani ni mahali halisi ambapo maumivu, huzuni, kifo na mabaya hayatainua pembe yake kamwe tena Nahum 1:9 .

Tumeshawahi kusikia mafungu au visa fulani vya Kitabu hiki kikuu ambacho ni kisima kisichokauka kwa kila mwanadamu. Biblia huchukua takribani masaa 80 kuisoma na kuimaliza, ila twahitaji muda wa kusali na kuimeng'enya. Tulipoanza kusoma na kujadili Biblia kama familia, sura kwa sura mwaka 2012, furaha yetu iliongezeka na sote tukaanza kukusanya visa hivyo vya Biblia 'kushare'; tukavihesabu na idadi ikawa 407. Watoto wetu walikuwa chini ya miaka 10 na walitoa mchango katika mijadala nasi tukaona tuviandike visa hivi kwa mfumo wa Kesha. Blogu ya UamshonaMatengenezoKiswahili inayosoma na kujadili sura moja ya Biblia Kila siku Kiswahili na Kingereza nazo zikatuongezea mengine. Hakika ukitaka kwenda haraka nenda peke yako ila ukitaka kwenda mbali nenda na wengine. Muhtasari wa Biblia ni Maneno Matatu tu, nayo ni Uumbaji, Maanguko na Ukombozi, ila NENO hili tutajifunza milele zote na hatutafikia kikomo chake. Utamu wake tutaumungunya taratibu milele zote na Viungo vyake vitazidi kuzama kwenye ulimi polepole, vikileta ladha tamu mno. Yeye ambaye Ni NENO Mwenyewe daima aliendelea kulisoma na kulitafakari japo Ndiye aliyelivuvia na kuliandika. Sisi je, tutaponaje basi tusipolijali NENO hili ambalo ndiyo Kweli, Uzima na Njia? Anza kusoma nasi leo! Haijalishi kama ni katikati ya mwaka, daima utapata tunu kubwa na mpya ambayo hutaisahau milele zote. Jiunge pamoja nasi kuombea watoto wetu, na kuombea uandishi wa Vitabu vya Watoto kwa Lugha zetu na Kijito cha Uvuvio ambayo ni Audio au Sikiliza ya kitabu hiki kwenye Youtube. Tunatamani mchango wenu!

Waandishi wamesomea fani za kemia, baolojia, Udaktari wa wanyama, unesi na Biblia na wameandika na kutafsiri vitabu kadhaa.


BWANA abariki watoto wote, wazee sote na watumishi nyote, tunapovisoma visa hivi tena na tena ili tuwe na Ibada na kicho cha Kweli tunapojiweka Wakfu tena kwa safari ya usomaji!

Grace na Daniel-Huduma ya Walei Wasamaria Uhamishoni, Ughaibuni, Mtandaoni na Nyumbani, Jersey, Marekani

Grace Momadi-Masaka na Daniel Masaka wanapenda kuyasoma Maandiko. Wamesomea fani za kemia, baolojia, Udaktari wa wanyama, unesi na Biblia na wameandika na kutafsiri vitabu kadhaa. Biblia ni kitabu kilichobadilisha maisha ya watu duniani kuliko kitabu kingine chochote kwa kuwa ni sauti ya MUNGU Mwenyewe iliyo na mamlaka ya mwisho duniani na mbinguni. Hakuna aliyesoma Kemia na kusema imemsaidia kuacha tabia ya uongo au dhambi. Neno la Mungu peke yake ndilo ambalo huleta tabia njema kwa watoto na watu wazima.

Walikuja kumwamini MUNGU kupitia unabii wa Danieli 2, wakiwa chini ya umri wa miaka 12. Unabii huu uliwaelezea kwamba Biblia inaendana na historia ya kweli ya mwanadamu iliyoanza Edeni na ambayo leo ipo kwenye mitaala ya shule na mitandao, nayo haizidi miaka 6000. Masihi katika Daniel 24:15 aliwahusia watu wasome unabiii huu. Asilimia 75 ya watoto wote humwamini Mwenyezi Mungu kama Muumbaji, Mdumishani na Mkombozi wao kabla ya kufika miaka 10! Na asilimia moja tu baada ya miaka 53! Lisome, Likariri, Litafakari, na Liishi NENO hili mchana na usiku. Nadharia zingine potofu kama uibukaji kwa kawaida huaminiwa na watu wazima zaidi, japo masimulizi yake ni ubunifu wa nchi za mbali zisizo na sokwe. Hii inatubidisha wazazi kuwalea watoto katika njia inayopasa nao wanapokuwa wazee hawataweza kuisahau, na siku moja watakuwa na Mwenyezi Mungu Mbinguni milele zote. Mbingu ni bure, tuombeane tusiikose kwani ni mahali halisi ambapo maumivu, huzuni, kifo na mabaya hayatainua pembe yake kamwe tena Nahum 1:9.

Tumeshawahi kusikia mafungu au visa fulani vya Kitabu hiki kikuu ambacho ni kisima kisichokauka kwa kila mwanadamu. Biblia huchukua takribani masaa 80 kuisoma na kuimaliza, ila twahitaji muda wa kusali na kuimeng'enya. Tulipoanza kusoma na kujadili Biblia kama familia, sura kwa sura mwaka 2012, furaha yetu iliongezeka na sote tukaanza kukusanya visa hivyo vya Biblia 'kushare'; tukavihesabu na idadi ikawa 407. Watoto wetu walikuwa chini ya miaka 10 na walitoa mchango katika mijadala nasi tukaona tuviandike visa hivi kwa mfumo wa Kesha. Blogu ya UamshonaMatengenezoKiswahili inayosoma na kujadili sura moja ya Biblia Kila siku Kiswahili na Kingereza nazo zikatuongezea mengine. Hakika ukitaka kwenda haraka nenda peke yako ila ukitaka kwenda mbali nenda na wengine. Muhtasari wa Biblia ni Maneno Matatu tu, nayo ni Uumbaji, Maanguko na Ukombozi, ila NENO hili tutajifunza milele zote na hatutafikia kikomo chake. Utamu wake tutaumungunya taratibu milele zote na Viungo vyake vitazidi kuzama kwenye ulimi polepole, vikileta ladha tamu mno. Yeye ambaye Ni NENO Mwenyewe daima aliendelea kulisoma na kulitafakari japo Ndiye aliyelivuvia na kuliandika. Sisi je, tutaponaje basi tusipolijali NENO hili ambalo ndiyo Kweli, Uzima na Njia? Anza kusoma nasi leo! Haijalishi kama ni katikati ya mwaka, daima utapata tunu kubwa na mpya ambayo hutaisahau milele zote. Jiunge pamoja nasi kuombea watoto wetu, na kuombea uandishi wa Vitabu vya Watoto kwa Lugha zetu na Kijito cha Uvuvio ambayo ni Audio au Sikiliza ya kitabu hiki kwenye Youtube. Tunatamani mchango wenu!



BWANA abariki watoto wote, wazee sote na watumishi nyote, tunapovisoma visa hivi tena na tena ili tuwe na Ibada na kicho cha Kweli tunapojiweka Wakfu tena kwa safari ya usomaji!

Grace na Daniel-Huduma ya Walei Wasamaria Uhamishoni, Ughaibuni, Mtandaoni na Nyumbani, Jersey, Marekani